# Biblia Takatifu

The Holy Bible in the Swahili language, Unlocked Literal Bible version

# Biblia Takatifu

## The Holy Bible in the Swahili language, Unlocked Literal Bible version

copyright © 2019 Door43 World Missions Community

Language: Kiswahili (Swahili)

Translation by: Door43 World Missions Community

Contributor: Alfred Danjuma, Bariki Malisa, Christina Abraham Kileo, Cloud Roman, Daniel Marura Chacha, Dina Mast, Dina Roman, Donald Shadarck Dutuyi, Emmanuel Masanja Mbaaga, Emmanuel Nyamalya, Erasmus Peter Malelo, Ev. Lazaro Chalomhola, Ezekiel Manala, Fred, Gabriel Gidale Merus, Gabriel Lwitakubi Mazige, James Makula, James Semnkai, Jeremiah Masasi, Jesse Katabi Masolwa, John Ojasi, Joyce Gilbert Masasi, Karen Riecks, Kazwanomo, Kennedy, Ker, Lameck Yakobo Tobotobo, Laurent Petro Malelo, Lazarus David Chalomhola, Makene Mafwele, Marco Luma Mahushi, Mathew Nkusa, Mathias William, Mr. James Semnkai .It., Musa Isaya Majama, Musa Luzali, Pastor John Kerim, Pastor Jordan, Philipo Mussa Kanwelle, Raphael Musa, Rev. Charles Mabisa, Rev. Yohana Batano, Robert Ndalahwa, Sadiki Kulwa, Samson Nungwana, Thobias Kazwanomo, Yohana Dutuyi, Yohana Magera, Zelote Loilang'akaki Lukumay, Rev. Erasmus Peter Malelo, Ev. Mathew Kazimoto, Rev. Dr. David Magoke, Rev. Elias Ndema, Rev. Alex Nyuri, Rev. Gungutu Elias, Rev. Lameck Tobotobo, Rev. Catherin D. Matia, Rev. Yohana S Dutuyi, Rev. Donald Dutuyi, GS. Andrew Gewe, Ev. Ezekiel Daudi, Rev. John Ndaluka, Ev. Moses Malugu, Rev. Moses Eliakim Ndege, Past. Isack A. Gomugo, Past. Mathias William, Rev. Yekonia M. Koko, Rev. Elisande Mhanga, Ev. James A. Makula

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

- You include the above copyright and source information.
- If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.
- If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2021-03-16

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 25 Aug 2023 from source files dated 11 Jun 2020
604b3af0-f37b-5180-9465-1911f927b37d

Contents


Mwanzo . . . 1
Kutoka . . . 53
Mambo ya Walawi . . . 97
Hesabu . . . 132
Kumbukumbu la Torati . . . 177
Yoshua . . . 215
Waamuzi . . . 242
Ruth . . . 267
1Samweli . . . 271
2 Samweli . . . 306
1Wafalme . . . 334
2 Wafalme . . . 368
1 Mambo ya Nyakati . . . 402
2 Mambo ya Nyakati . . . 431
Ezra . . . 470
Nehemia . . . 480
Esta . . . 495
Ayubu . . . 503
Zaburi . . . 533
Mithali . . . 600
Mhubiri . . . 623
Wimbo wa Sulemani . . . 632
Isaya . . . 637
Yeremia . . . 687
Maombolezo . . . 745
Ezekieli . . . 750
Danieli . . . 804
Hosea . . . 821
Joeli . . . 829
Amosi . . . 832
Obadia . . . 838
Yona . . . 839
Mika . . . 841
Nahumu . . . 846
Habakuki . . . 849
Sefania . . . 852
Hagai . . . 855
Zekaria . . . 857
Malaki . . . 866
Mathayo . . . 869
Marko . . . 903
Luka . . . 924
Yohana . . . 961
Matendo ya Mitume . . . 989
Warumi . . . 1024
1 Wakorintho . . . 1039
2 Wakorintho . . . 1053
Wagalatia . . . 1063

Waefeso . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1068
Wafilipi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1073
Wakolosai . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1077
1 Wathesalonike . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1081
2 Wathesalonike . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1084
1Timotheo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1086
2 Timotheo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1090
Tito . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1093
Filemoni . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1095
Wahebrania . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1096
Waraka wa Yakobo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1108
1 Petro . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1112
2 Petro . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1116
1Yohana 1 . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1119
2 Yohana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1123
3 Yohana . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1124
Yuda . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1125
Ufunuo . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1127

# Mwanzo

1 Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi. 2 Nayo nchi haikuwa na umbo na
ilikuwa tupu. Giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji. Roho wa Mungu alikuwa
akielea juu ya uso wa maji. 3 Mungu akasema, "na kuwe nuru," na kulikuwa na
nuru. 4 Mungu akaona nuru kuwa ni njema. Akaigawa nuru na giza. 5 Mungu akaiita
nuru " mchana" na giza akaliita "usiku." Ikawa jioni na asubuhi, siku ya kwanza.
6 Mungu akasema, " na kuwe na anga kati ya maji, na ligawe maji na maji." 7 Mungu
akafanya anga na kugawanya maji yaliyo kuwa chini ya anga na maji ambayo
yalikuwa juu ya anga. Ikawa hivyo. 8 Mungu akaita anga "mbingu." Ikawa jioni
na asubuhi siku ya pili. 9 Mungu akasema, "maji yaliyo chini ya mbingu yakusanyike
pamoja mahali pamoja, na ardhi kavu ionekane." Ikawa hivyo. 10 Mungu aliita
ardhi kavu "nchi," na maji yaliyo kusanyika akayaita "bahari." Akaona kuwa ni
vyema. 11 Mungu akasema, nchi ichipushe mimea: miche itoayo mbegu na miti ya
matunda itoayo matunda ambayo mbegu yake imo ndani ya tunda, kila kitu kwa
namna yake." Ikawa hivyo. 12 Nchi ikatoa mimea, miche itoayo mbegu ya aina yake,
na miti itoayo tunda ambalo mbegu yake imo ndani yake, kwa aina yake. Mungu
akaona kuwa ni vyema. 13 Ikawa jioni na asubuhi, siku ya tatu. 14 Mungu akasema,
"kuwe na mianga katika anga kutenganisha mchana na usiku. Na ziwe kama ishara,
kwa majira, kwa siku na miaka. 15 Ziwe mianga katika anga ili kutoa mwanga juu
ya nchi." Ikawa hivyo. 16 Mungu akafanya mianga mikuu miwili, mwanga mkuu
zaidi kutawala mchana, na mwanga mdogo kutawala usiku. Akafanya nyota pia.
17 Mungu akazipanga katika anga kutoa mwanga juu nchi, 18 kutawala mchana na
usiku, na kugawanya mwanga kutoka kwenye giza. Mungu akaona kuwa ni vyema.
19 Ikawa jioni na asubuhi, siku ya nne. 20 Mungu akasema, "maji yajae idadi kubwa
ya viumbe hai, na ndege waruke juu ya nchi katika anga la mbingu." 21 Mungu
akaumba viumbe wakubwa wa baharini, pamoja na kila kiumbe hai cha aina yake,
viumbe waendao na wanaojaa kila mahali majini, na kila ndege mwenye mabawa
kwa aina yake. Mungu akaona kuwa ni vyema. 22 Mungu akavibariki, akisema,
"zaeni na muongezeke, na mjae majini katika bahari. Ndege waongezeke juu nchi."
23 Ikawa jioni na asubuhi, siku ya tano. 24 Mungu akasema, " nchi na itoe viumbe hai,
kila kiumbe kwa aina yake, mnyama wa kufugwa, vitu vitambaavyo, na wanyama
wa nchi, kila kitu kwa jinsi yake." Ikawa hivyo. 25 Mungu akafanya wanyama wa
nchi kwa aina yake, wanyama wa kufugwa kwa aina yake, na kila kitambaaho juu
ya ardhi kwa aina yake. Akaona kuwani vyema. 26 Mung akasema, "na tumfanye
mtu katika mfano wetu, wa kufanana na sisi. Wawe na mamlaka juu ya samaki wa
bahari, juu ya ndege wa angani, juu ya wanyama wa kufuga, juu ya nchi yote, na
juu ya kila kitu kitambaacho kinacho tambaa juu ya nchi." 27 Mungu akamuumba
mtu kwa mfano wake. Katika mfano wake alimuumba. Mwanaume na mwanamke
aliwaumba. 28 Mungu akawabariki na akawaambia, "zaeni na kuongezeka. Jazeni
nchi, na muitawale. Muwe na mamlaka juu ya samaki wa baharini, juu ya ndege
wa angani, na juu ya kila kiumbe hai kiendacho juu ya nchi," 29 Mungu akasema,
"tazama, nimewapeni kila mmea uzaao mbegu ambao uko juu ya nchi, na kila mti
wenye tunda ambalo lina mbegu ndani yake. Vitakuwa ni chakula kwenu. 30 Kwa
kila mnyama wa nchi, kwa kila ndege wa angani, na kila kitambaacho juu ya nchi, na
kila kiumbe ambacho kina pumzi ya uhai ni metoa kila mmea kwa ajili ya chakula."
ikawa hivyo. 31 Mungu akaona kila kitu alichokiumba. Tazama, kikawa chema sana.
Ikawa jioni na asubuhi siku ya sita.

# 2

1 Kisha mbingu na nchi zilimalizika, na viumbe hai vyote vilivyo jaza mbingu na
nchi. 2 Siku ya saba Mungu alifikia mwisho wa kazi yake ambayo aliifanya, na kwa
hiyo alipumzika siku ya saba kutoka kwenye kazi yake yote. 3 Mungu akaibarikia siku
ya saba na akaitakasa, kwa sababu katika siku hiyo alipumzika kutoka kwenye kazi
yake yote ambayo aliifanya katika uumbaji. 4 Haya yalikuwa ni matukio yahusuyo
mbingu na nchi, wakati vilipoumbwa, katika siku ambayo Yahwe Mungu aliumba
nchi na mbingu. 5 Hapakuwa na msitu wa shambani uliokuwa katika nchi, na
hapakuwa na mmea wa shambani uliokuwa umechipuka, kwa kuwa Yahwe Mungu
alikuwa hajasababisha mvua kunyesha juu ya nchi, na hapakuwa na mtu wa kulima
ardhi. 6 Lakini ukungu uliinuka juu kutoka kwenye nchi na kuutia maji uso wote wa
ardhi. 7 Yahwe Mungu aliumba mtu kutoka mavumbi ya ardhi, na akampulizia puani
pumzi ya uhai, na mtu akawa kiumbe hai. 8 Yahwe Mungu aliotesha bustani upande
wa mashariki, katika Edeni, na pale akamuweka mtu ambaye alimuumba. 9 Kutoka
ardhini Yahwe Mungu alifanya kila mti uote ambao unapendeza na ni mzuri kwa
chakula. Hii ni pamoja na mti wa uzima ambao ulikuwa katikati ya bustani, na mti
wa ujuzi wa mema na mabaya. 10 Mto ukatoka nje ya Edeni kuitia maji bustani.
Na kutoka pale ukagawanyika na kuwa mito minne. 11 Jina la ule wa kwanza ni
Pishoni. Huu ni ule ambao unatiririka kupitia nchi yote ya Havila, ambapo kuna
dhahabu. 12 Dhahabu ya inchi ile ni nzuri. pia kuna bedola na jiwe shohamu. 13 Jina
la mto wa pili ni Gihoni. Huu unatiririka kupitia nchi yote ya kushi. 14 Jina la
mto wa tatu ni Hidekeli, ambao unatiririka mashariki mwa Ashuru. Mto wa nne
ni Frati. 15 Yahwe Mungu alimtwaa mtu na kumweka ndani ya bustani ya Edeni
kuilima na kuitunza. 16 Yahwe Mungu alimuagiza mtu akisema, "kutoka kwenye
kila mti bustanini waweza kula kwa uhuru. 17 Lakini kutoka kwenye mti wa ujuzi
wa mema na mabaya usile, kwa kuwa siku utakayo kula kutoka katika mti huo,
utakufa hakika." 18 Kisha Yahwe Mungu akasema, "siyo jambo jema kwamba mtu
huyu lazima awe pekeyake. Nitamfanyia msaidizi anaye mfaa." 19 Kutoka ardhini
Yahwe Mungu akafanya kila mnyama wa kondeni na kila ndege wa angani. Kisha
akawaleta kwa mtu huyu aone angewapatia majina gani. Jina ambalo mtu huyu
alimwita kila kiumbe hai, hili ndilo lilikuwa jina lake. 20 Mtu huyu akawapatia majina
wanyama wote, ndege wote wa angani, na kila mnyama wa mwitu. Lakini kwa mtu
mwenyewe hapakuwa na msaidizi wa kumfaa yeye. 21 Yahwe Mungu akaleta usingizi
mzito kwa mtu huyu, kwa hiyo mtu huyu akalala. Yahwe Mungu akatwaa moja ya
mbavu za mtu huyu na akapafunika pale alipo chukua ubavu. 22 Kwa ubavu ambao
Yahwe Mungu alichukua toka kwa mtu huyu, akafanya mwanamke na akamleta
kwa mtu huyu. 23 Mwanaume akasema, "kwa sasa, huyu ni mfupa katika mifupa
yangu, na nyama katika nyama yangu. ataitwa 'mwanamke,' kwa sababu ametwaliwa
katika mwanaume. 24 Kwa hiyo mwanaume atawaacha baba yake na mama yake,
ataungamanika na mke wake, na watakuwa mwili mmoja. 25 Wote wawili walikuwa
uchi, mwanaume na mke wake, lakini hawakuona aibu.

# 3

1 Sasa nyoka alikuwa mwerevu kuliko myama mwingine yeyote wa kondeni
ambaye Yahwe Mungu alikuwa amemuumba. Akamwambia mwanamke, "Je ni
kweli Mungu amesema, 'Msile matunda kutoka kwenye mti wowote bustanini'?"
2 Mwanamke akamwambia nyoka, "Twaweza kula tunda kutoka kwenye miti ya
bustani, 3 lakini kuhusu tunda la mti ambao uko katikati ya bustani, Mungu alisema,
'msile, wala msiuguse, vinginevyo mtakufa.'" 4 Nyoka akamwambia mwanamke,
"hakika hamtakufa. 5 Kwasababu Mungu anajua kwamba siku mkila macho yenu

yatafumbuliwa, na mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya." 6 Na
mwanamke alipoona kuwa mti ni mzuri kwa chakula, na kuwa unapendeza macho,
na kwamba mti ulitamanika kwa kumfanya mtu awe mwerevu, alichukua sehemu
ya tunda na akala. Na sehemu yake pia akampatia mumewe aliyekuwa naye,
naye akala. 7 Macho ya wote wawili yalifumbuliwa, na wakajua kuwa wako uchi.
Wakashona majani ya miti pamoja na wakatengeneza vya kujifunika wao wenyewe.
8 Wakasikia sauti ya Yahwe Mungu akitembea bustanini majira ya kupoa kwa jua,
kwa hiyo mwanaume na mke wake wakajificha wao wenyewe kwenye miti ya
bustani kuepuka uwepo wa Yahwe Mungu. 9 Yahwe Mungu akamuita mwanaume
na kumwambia, " uko wapi?" 10 Mwanaume akasema, "nilikusikia bustanini, na
nkaogopa, kwa sababu nilikuwa uchi. kwa hiyo nikajificha." 11 Mungu akasema, "Ni
nani alikwambia kuwa ulikuwa uchi? Je umekula kutoka mti ambao nilikuagiza
usile matunda yake?" 12 Mwanaume akasema, " Mwanamke uliyenipa kuwa na
mimi, alinipatia tunda kutoka kwenye mti, na nikala." 13 Yahwe Mungu akamwambia
mwanamke, " Nini hiki ulichofanya?" mwanamke akasema, "nyoka alinidanganya,
na nikala." 14 Yahwe Mungu akamwambia nyoka, " kwa sababu umefanya jambo
hili, umelaaniwa wewe mwenyewe miongoni mwa wanyama wote wa kufugwa na
wanyama wote wa mwituni. Itakuwa kwa tumbo lako utakwenda, na mavumbi
utakula kwa siku zote za maisha yako. 15 Nitaweka uadui kati yako na mwanamke, na
kati ya uzao wako na uzao wake. Atakujeruhi kichwa chako na utamjeruhi kisigino
chake." 16 Kwa mwanamke akasema, nitaongeza uchungu wakati wa kuzaa watoto;
itakuwa katika maumivu utazaa watoto. Tamaa yako itakua kwa mume wako, lakini
atakutawala." 17 Kwa Adam akasema, "kwa sababu umesikiliza sauti ya mke wako,
na umekula kutoka katika mti, ambao nilikuagiza, nikisema, " usile matunda yake',
ardhi imelaaniwa kwa sababu yako; kupitia kazi yenye maumivu utakula matunda ya
ardhi kwa siku zote za maisha yako. 18 Ardhi itazaa miiba na mbigili kwa ajili yako,
na utakula mimea ya shambani. 19 Kwa jasho la uso wako utakula mkate, mpaka
utakapo irudia ardhi, ambayo kwayo ulitwaliwa. kwa kuwa wewe ni mavumbi na
kwenye mavumbi utarudi." 20 Mwanaume akaita mke wake jina Hawa kwa sababu
alikuwa mama wa wote wenye uhai. 21 Yahwe Mungu akatengeneza mavazi ya ngozi
kwa ajili ya Adam na mke wake na akawavalisha. 22 Yahwe Mungu akasema, " sasa
mtu huyu amekuwa kama mmoja wetu, ajuaye mema na mabaya. Kwa hiyo sasa
hataruhusiwa kugusa kwa mkono wake, na kuchukua tunda la mti wa uzima, na kula
akaishi tena milele." 23 Kwa hiyo Yahwe Mungu akamuondoa kutoka kwenye bustani
ya Edeni, kwenda kulima ardhi ambayo kwahiyo alikuwa ametwaliwa. 24 Kwa hiyo
Mungu akamfukuza mtu huyu nje ya bustani, na akaweka kerubi mashariki mwa
bustani ya Edeni, na upanga wa moto ulio geuka geuka kila upande, ili kulinda njia
ya kwenda kwenye mti wa uzima.

# 4

1 Mwanume akalala na Hawa mke wake. Akabeba mimba na akamzaa Kaini.
Akasema, " nimezaa mwanaume kwa msaada wa Yahwe." 2 Kisha akazaa ndugu
yake Habili. Sasa Habili akawa mchungaji, lakini Kaini alilima udongo. 3 Ikawa
kwamba baada ya muda Kaini alileta sehemu ya mazao ya ardhi kama sadaka kwa
Yahwe. 4 Habili pia, alileta sehemu ya wazao wa kwanza wa wanyama wake na
sehemu zilizonona. Yahwe akamkubali Habili pamoja na sadaka yake, 5 lakini Kaini
pamoja na sadaka yake Mungu hakuikubali. Kwa hiyo Kaini alikasirika sana, na
uso wake ukakunjamana. 6 Yahwe akamwambia Kaini, " kwa nini umekasirika na
kwa nini uso wako umekunjamana? 7 Kama ukifanya vema, je hutapata kibali? lakini
kama hutafanya lilio jema, dhambi iko inakuotea mlangoni na inatamani kukutawala,

lakini inakupasa uishinde. 8 Kaini akamwambia Habili ndugu yake. Hata wakati
walipokuwa shambani, Kaini aliinuka dhidi ya Habili ndugu yake na akamuua.
(Katika tafsiri za kale zinasema, Kaini alimwambia Habili ndugu yake, “ twende
mashambani.” Na wakati walipokuwa shambani, Kaini alimuinukia Habili ndugu
yake na kumuua). 9 Kisha Yahwe akamuuliza Kaini, “Ndugu yako Habili yuko wapi?”
Akasema, “sijui. Je mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?” 10 Yahwe akasema, “umefanya
nini? damu ya ndugu yako inaniita mimi kutokea ardhini. 11 Na sasa umelaaniwa
wewe kutoka ardhi ambayo imefungua kinywa chake kupokea damu ya ndugu yako
kutoka mikononi mwako. 12 Utakapo ilima ardhi, kuanzia sasa na kuendelea haita
kuzalia wewe nguvu yake. Utakuwa mkimbizi na mtu asiye na makao duniani.”
13 Kaini akamwambia Yahwe, “Adhabu yangu ni kubwa kuliko uwezo wangu wa
kustahimili. 14 Kwa hakika umenifukuza siku hii ya leo kutoka kwenye ardhi hii,
na sitaonekana mbele ya uso wako. Nitakuwa mkimbizi na mtu nisiye na makao
katika dunia, na yeyote atakaye niona ataniua.” 15 Yahwe akamwambia, “ikiwa
mtuyeyote atamuua Kaini, kisasi kitakuwa juu yake mara saba.” Kisha Yahwe
akaweka alama juu ya Kaini, ili kwamba kama mtu awayeyote akimuona, mtu huyo
asimshambulie. 16 Kwa hiyo Kaini akatoka mbele ya uwepo wa Yahwe na akaishi
katika nchi ya Nodi, mashariki mwa Edeni. 17 Kaini akamjua mke wake na akapata
mimba. Akamzaa Henoko. Akajenga mji na akauita kwa jina la mwanae Henoko.
18 Kwa Henoko akazaliwa Iradi. Iradi akamzaa Mehuyaeli. Mehuyaeli akamzaa
Methushaeli. Methushaeli akamzaa Lameki. 19 Lameki akajitwalia wake wawili:
jinala mmoja alikuwa Ada, na jina la yule mwingine alikuwa Sila. 20 Ada akamzaa
Yabali. Huyu ndiye alikuwa baba yao na wale walioishi hemani ambao wanafuga
wanyama. 21 Ndugu yake aliitwa Yubali. Huyu alikuwa baba yao na wale wapigao
kinubi na filimbi. 22 Sila naye akamzaa Tubal Kaini, mfua vyombo vya shaba na
chuma. Dada yake na Tubal Kaini alikuwa Naama. 23 Lameki akawaambia wake
zake, Ada na Sila, sikieni sauti yangu; ninyi wake wa Lameki, sikilizeni nisemacho.
Kwa kuwa nimemuua mtu kwa kunijeruhi, kijana kwa kunichubua. 24 Ikiwa Kaini
atalipiwa kisasi mara saba, ndipo Lameki atalipiwa kisasi mara sabini na saba.”
25 Adam akamjua mke wake tena, na akazaa mtoto mwanaume. Akamuita jina
lake Sethi na akasema, “ Mungu amenipatia mtoto mwingine wa kiume kwa nafasi
ya Habili, kwa kuwa Kaini alimuuwa.” 26 Mtoto wa kiume alizaliwa kwa Sethi na
akamuita jina lake Enoshi. Wakati huo watu walianza kuliitia jina la Yahwe.

# 5

1 Hii ni orodha ya vizazi vya Adamu. Katika siku ambayo Mungu alimuumba mtu,
aliwaumba katika mfano wake mwenyewe. 2 Mwanaume na mwanamke aliwaumba.
Akawabariki na akawaita Adam wakati walipoumbwa. 3 Wakati Adamu alipokuwa
ameishi miaka 130, akamzaa mwana katika sura yake mwenyewe, kwa mfano wake,
na akamuita jina lake Sethi. 4 Baada ya Adamu kumzaa Sethi, aliishi miaka mia
nane. Akawazaa wana wengi waume na wake. 5 Adamu akaishi miaka 930 kisha
akafariki. 6 Wakati Sethi alipokuwa ameishi miaka 105, akamzaa Enoshi. 7 Baada ya
kumzaa Enoshi, akaishi miaka 807 na akawazaa wana wengi waume na wake. 8 Sethi
akaishi miaka 912 kisha akafariki. 9 Wakati Enoshi alipokuwa ameishi miaka tisini,
akamzaa Kenani. 10 Baada ya kumzaa Kenani, Enoshi aliishi miaka 815. Akazaa
wana wengi wa ume na wake. 11 Enoshi aliishi miaka 905 na kisha akafariki.
12 Wakati Kanani alipokuwa ameishi miaka sabini, akamzaa Mahalaleli. 13 Baada
ya kumzaa Mahalaleli, Kenani aliishi miaka 840. Akawazaa wana wengi wa ume
na wake. 14 Kenani aliishi miaka 910, na kisha akafariki. 15 Mahalaleli alipokuwa
ameishi miaka sitini na tano, alimzaa Yaredi. 16 Baada ya kumzaa Yaredi, Mahalaleli

aliishi miaka 830. Akazaa wana wengi wa ume na wake. [17] Mahalaleli aliishi miaka
895 na kisha akafariki. [18] Yaredi alipokuwa ameishi miaka 162, alimzaa Henoko.
[19] Baada ya kumzaa Henoko, Yaredi aliishi miaka mianane. Akazaa wana wengi
waume na wake. [20] Yaredi aliishi miaka 962 na kisha akafariki. [21] Henoko alipokuwa
ameishi miaka sitini na tano, akamzaa Methusela. [22] Henoko akaenenda na Mungu
miaka miatatu baada ya kumzaa Methusela. Aliwazaa wana wengi wa ume na wake.
[23] Henoko aliishi miaka 365. [24] Henoko alienenda na Mungu, na kisha alitoweka, kwa
kuwa Mungu alimtwaa. [25] Wakati Methusela alipokuwa ameishi miaka 187, alimzaa
Lameki. [26] Baada ya kumzaa Lameki, Methusela aliishi miaka 782. Akawazaa wana
wengi wa ume na wake. [27] Methusela aliishi miaka 969. Kisha akafariki. [28] Wakati
Lameki alipokuwa ameishi miaka 182, alimzaa mwana. [29] Akamuita jina lake Nuhu,
akisema, "Huyu ndiye atatupatia pumziko kutoka katika kazi yetu na kutoka katika
kazi ya taabu ya mikono yetu, ambayo lazima tuifanye kwa sababu ya ardhi ambayo
Yahwe ameilaani." [30] Lameki aliishi miaka 595 baada ya kumzaa baba wa Nuhu.
Akazaa wanawengi wa ume na wake. [31] Lameki aliishi miaka 777. Kisha akafariki.
[32] Baada ya Nuhu kuishi miaka miatano, akamzaa Shemu, Hamu, na Yafethi.

# 6

[1] Ikawa wakati watu walipoanza kuongezeka juu ya uso wa nchi na wana wa
kike wakazaliwa kwao, [2] wana wa Mungu walipoona kuwa mabinti wa wanadamu
ni wenye kuvutia. waliwachukua kuwa wake zao, kila waliye mchagua. [3] Yahwe
akaema, " roho yangu haitasalia kwa mwanadamu milele, kwa kuwa wao ni nyama.
Wataishi miaka 120." [4] Majitu makubwa yalikuwa juu ya uso wa nchi nyakati hizo,
na hata baada ya hapo. Hii ilitokea wakati wana wa Mungu walipowaoa binti za
wanadamu, na kupata watoto pamoja nao. Hawa walikuwa watu hodari zamani,
watu wenye sifa. [5] Yahwe akaona kwamba uovu wa watu umezidi katika nchi, na
kwamba mawazo ya mioyo yao daima inaelekea tu katika uovu. [6] Yahwe akajuta
kuwa amemuumba mwanadamu juu ya nchi, na ikamuhuzunisha moyo wake. [7] Kwa
hiyo Yahwe akasema, "Nitamfutilia mbali mwanadamu ambaye nimemuumba katika
uso wa nchi; mwanadamu na wanyama wakubwa, na vitambaavyo na ndege wa
angani, kwa kuwa nimehuzunika kuwa nimeviumba." [8] Lakini Nuhu akapata neema
ya upendeleo machoni pa Yahwe. [9] Kulikuwa na matukio kumuhusu Nuhu. Nuhu
alikuwa mtu mwenye haki, na asiye na lawama miongoni mwa watu wa kipindi
chake. Nuhu alitembea na Mungu. [10] Nuhu akafanyika baba wa wana watatu wa
kiume: Shem, Ham na Yafeti. [11] Nchi iliharibika mbele za Mungu, na ikajaa ghasia.
[12] Mungu akaiona nchi; tazama, ilikuwa imeharibika, kwa kuwa wote wenye mwili
walikuwa wameharibu njia zao juu ya nchi. [13] Mungu akamwambia Nuhu, "Nimeona
kuwa sasa niwakati wa mwisho kwa wote wenye mwili, kwa kuwa inchi imejaa
ghasia kutokana na wao. Hakika, nitawaharibu wao pamoja na nchi. [14] Tengeneza
safina ya mti wa mvinje kwa ajili yako. Tengeneza vyumba katika safina, na vifunike
kwa lami ndani na nje. [15] Hivi ndivyo utakavyofanya: urefu wa safina dhiraa miatatu,
upana wake dhiraa hamsini, kwenda juu kwake dhiraa thelathini. [16] Tengeneza paa
la safina, na ulimalize kwa kipimo cha dhiraa kutoka juu ubavuni. Weka mlango
katika ubavu wa safina na utengeneze dari ya chini, ya pili na ya tatu. [17] Sikiliza,
nimekaribia kuleta gharika ya maji juu ya nchi, kuharibu wenye mwili wote wakaao
ndani ya nchi wenye pumzi ya uhai chini ya mbingu. Kila kitu kilichopo juu ya nchi
kitakufa. [18] Lakini nitalifanya thabiti agano langu na wewe. Utaingia ndani ya safina,
wewe, na wana wako wa kiume, na mke wako, pamoja na wake za wanao. [19] Kwa kila
kiumbe hai chenye mwili, viwili vya kila aina utavileta ndani ya safina, ili visalie hai
pamoja nawe, vya kike na vya kiume. [20] Katika ndege kwa jinsi yake, na wanyama

wakubwa kwa jinsi yake, kila kitambaacho ardhini kwa jinsi yake, viwili viwili vya
kila aina vitakuja kwako ili viwe salama. 21 Kusanya kila aina ya chakula kinacholiwa
kwa ajili yako na ukitunze, ili kwamba viwe chakula chako na chao." 22 Kwa hiyo
Nuhu akafanya hivi. kulingana na yote ambayo Mungu alimuagiza, ndivyo alifanya.

## 7

1 Yahwe akamwambia Nuhu, "Njoo, wewe na nyumba yako wote, katika safina, kwa
kuwa nimeona kuwa wewe ni mwenye haki mbele yangu katika kizazi hiki. 2 Kwa
kila mnyama aliye safi utakuja nao saba wa kiume na saba wa kike. Na kwa wanyama
wasio safi, lete wawili wawili, wakiume na wakike. 3 Pia na kwa ndege wa angani,
lete saba wa kiume na saba wa kike, ili kuhifadhi kizazi chao juu ya uso wa nchi yote.
4 Kwa kuwa ndani ya siku saba nitasababisha mvua kunyesha juu ya nchi muda wa
siku arobaini mchana na usiku. Nitaharibu kila kiumbe hai nilichokiumba juu ya
uso wa ardhi." 5 Nuhu alifanya yote ambayo Yahwe alimuagiza. 6 Nuhu alikuwa
na umri wa miaka mia sita wakati gharika ilipokuja juu ya nchi. 7 Nuhu, watoto
wake wa kiume, mke wake, na wake za watoto wake waliingia katika safina pamoja
kwa sababu ya maji ya gharika. 8 Wanyama ambao ni safi na wanyama ambao si
safi, ndege, na kila kitambaacho juu ya ardhi, 9 wawili wawili mume na mke wakaja
kwa Nuhu na wakaingia katika safina, kama vile Mungu alivyokuwa amemwagiza
Nuhu. 10 Ikawa kwamba baada ya siku saba, maji ya gharika yakaja juu ya nchi.
11 Katika mwaka wa mia sita wa maisha yake Nuhu, katika mwezi wa pili, katika
siku ya kumi na saba ya mwezi, katika siku iyo hiyo, chemchemi zote za vilindi
vikuu zilipasuka na kufunguka, na madirisha ya mbinguni yakafunguka. 12 Mvua
ikaanza kunyesha juu ya nchi kwa siku arobaini mchana na usiku. 13 Katika siku
iyo hiyo Nuhu pamoja na watoto wake, Shem, Ham, na Yafethi na mke wa Nuhu, na
wale wake watatu wa wana wa Nuhu pamoja waliingia katika safina. 14 Waliingia
pamoja na kila mnyama wa mwitu kwa jinsi yake, na kila mnyama wa kufugwa
kwa jinsi yake, na kila kitambaacho juu ya ardhi kwa jinsi yake, na kila aina ya
ndege kwa jinsi yake, kila aina ya kiumbe chenye mabawa. 15 Viwili viwili katika
kila chenye mwili ambacho kilikuwa na pumzi ya uhai kilikuja kwa Nuhu na kuingia
katika safina. 16 Wanyama walioingia ndani walikuwa wakiume na kike katika wote
wenye mwili; wakaingia kama vile Mungu alivyokuwa amemwagiza. Kisha Yahwe
akawafungia mlango. 17 Kisha gharika ikaja juu ya nchi kwa siku arobaini, na maji
yakaongezeka na kuinua safina juu ya nchi. 18 Maji yakafunika kabisa nchi, na
safina ikaelea juu ya uso wa maji. 19 Maji yakaongezeka zaidi juu ya nchi kiasi
kwamba milima yote mirefu ambayo ilikuwa chini ya anga ikafunikwa. 20 Maji
yakaongezeka dhiraa kumi na tano juu ya vilele vya milima. 21 Vitu vyote vyenye
uhai ambavyo vilitembea juu ya nchi vilikufa: ndege, mifugo, wanyama wa mwituni,
viumbe hai vyote kwa wingi vilivyoishi juu ya nchi, pamoja na watu. 22 Viumbe
hai vyote ambavyo vilikaa juu ya ardhi, vilivyo pumua pumzi ya uhai kwa njia ya
pua, vilikufa. 23 Hivyo kila kilichokuwa hai ambacho kilikuwa juu ya uso wa mchi
kilifutwa, kuanzia watu mpaka wanyama wakubwa, mpaka vitambaavyo, na mpaka
ndege wa angani. Vyote viliangamizwa kutoka kwenye nchi. Nuhu tu pamoja na
wale waliokuwa naye kwenye safina ndio walisalia. 24 Maji haya kuzama chini ya
nchi kwa muda wa siku miamoja na hamsini.

## 8

1 Mungu akamtazama Nuhu, wanyama wote wa mwitu, na wanyama wote wa
kufugwa ambao walikuwa pamoja naye kwenye safina. Mungu akafanya upepo
uvume juu ya nchi, na maji yakaanza kuzama chini. 2 Chemichemi za vilindi pamoja

na madirisha ya mbingu vikafungwa, na mvua ikakoma kunyesha. 3 Maji ya gharika
yakaanza kuzama kidogo kidogo katika nchi. na mwisho wa siku miamoja na hamsini
maji yakawa yamezama chini. 4 safina ikatulia katika mwezi wa saba, siku ya kumi
na saba ya mwezi, juu ya milima ya Ararati. 5 Maji yakaendelea kuzama chini
hadi mwezi wa kumi. Siku ya kwanza ya mwezi, vilele vya milima vikaonekana.
6 Ikatokea kwamba baada ya siku arobaini Nuhu alifungua dirisha la safina ambayo
aliitengeneza. 7 Akatuma kunguru na akaruka hadi maji yalipo kauka katika nchi.
8 Kisha akatuma njiwa kuona kama maji yamezama chini kutoka kwenye uso wa
nchi, 9 lakini njiwa hakuona sehemu ya kutua unyayo wake, na akarudi kwake ndani
ya safina, kwa kuwa maji yalikuwa bado yamefunika nchi yote. Akanyoosha mkono
wake, akamchukua na kumuweka ndani ya safina pamoja naye. 10 Akasubiri siku
saba zingine akatuma tena njiwa kutoka kwenye safina. 11 Njiwa akarudi kwake jioni.
Tazama! katika mdomo wake kulikuwa na jani bichi la mzeituni lililochumwa. Kwa
hiyo Nuhu akatambua kuwa maji yamekwisha zama chini ya nchi. 12 Akasubiri siku
saba zingine na akamtuma njiwa tena. Njiwa hakurudi kwake tena. 13 Ikawa kwamba
katika mwaka wa mia sita na moja, katika mwezi wa kwanza, siku ya kwanza
ya mwezi, maji yalikuwa yamekauka katika nchi. Nuhu akaondoa kifuniko cha
safina, akatazama nje, na akaona kwamba, Tazama, uso wa nchi ulikuwa umekauka.
14 Katika mwezi wa pili, siku ya ishirini na saba ya mwezi, nchi ilikuwa imekauka.
15 Mungu akamwambia Nuhu, 16 “Toka nje ya safina, wewe, mke wako, wanao wa
kiume, na wake wa wanao pamoja nawe. 17 Wachukuwe utoke nje pamoja nao kila
kiumbe hai chenye mwili ambacho kiko nawe - ndege, wanyama wa kufugwa, na kila
kitambaacho ambacho hutambaa juu ya nchi - ili kwamba viweze kukua na kuwa na
idadi kubwa zaidi ya viumbe hai katika nchi yote, kwa kuzaliana na kuongezeka juu
ya nchi.” 18 Kwa hiyo Nuhu akatoka nje pamoja na watoto wake wa kiume, mke wake,
na wake wa wa wanawe pamoja naye. 19 Kila kiumbe hai, kila kitambaacho, na kila
ndege, na kila kiendacho juu ya nchi, kwa kabila zao, wakaiacha safina. 20 Nuhu
akajenga madhabahu kwa Yahwe. Akachukua baadhi ya wanyama walio safi na
baadhi ya ndege walio safi, na kutoa sadaka ya kuteketezwa juu ya madhabahu.
21 Yahwe akanusa harufu nzuri ya kuridhisha na akasema moyoni mwake, “ Sita
laani tena ardhi kwa sababu ya mwanadamu, ingawa nia za mioyo yao ni mbaya
tokea utoto. Wala sita haribu kilakitu chenye uhai, kama nilivyo fanya. 22 Wakati nchi
isaliapo, majira ya kupanda mbegu na mavuno, baridi na joto, kiangazi na majira ya
baridi, mchana na usiku havitakoma.”

# 9

1 Kisha Mungu akambariki Nuhu na wanawe, na kuwaambia, “Zaeni, mkaongezeke,
na muijaze nchi. 2 Hofu na utisho wenu vitakuwa juu ya kila mnyama aliye hai juu
ya nchi, juu ya kila ndege wa angani, juu ya kila kitu kiendacho chini juu ya ardhi,
na juu ya samaki wote wa baharini. Vimetolewa katika mikono yenu. 3 Kila kitu
kiendacho kilicho hai kitakuwa chakula kwa ajili yenu. Kama nilivyo wapa mimea,
sasa nawapa kila kitu. 4 Lakini msile nyama pamoja na uhai wake - yaani damu
yake - ndani yake. 5 Lakini kwa ajili ya damu yenu, uhai uliomo katika damu yenu
nitataka malipo. Kutoka katika mkono wa kila mnyama nitaitaka. Kutoka katika
mkono wa kila mtu, yaani, kutoka katika mkono wa yule ambaye amemuua ndugu
yake, nitataka fidia kwa ajili ya uhai wa mtu huyo. 6 Yeyote amwagaye damu ya
mtu, kwa njia ya mtu damu yake itamwagwa, kwa sababu ilikuwa ni katika mfano
wa Mungu kwamba Mungu alimuumba mtu. 7 Na hivyo nanyi zaeni na kuongezeka,
sambaeni katika inchi yote na muongezeke juu yake.” 8 Kisha Mungu akazungumza
na Nuhu na wanae pamoja naye, akisema, 9 “Kwa ajili yangu, sikiliza! Ninakwenda

kulithibitisha agano langu pamoja nawe na uzao wenu baada yenu, [10] na kwa kila
kiumbe hai kilicho pamoja nawe, pamoja na ndege, mnyama wa kufugwa, na kila
kiumbe cha nchi pamoja nawe, kuanzia kwa wote waliotoka kwenye safina, mpaka
kwa kila kiumbe hai juu ya nchi. [11] Kwa sababu hii ninalithibitisha agano langu
pamoja nanyi, kwamba hapatatokea kuangamizwa kwa mwenye mwili kwa njia ya
maji ya gharika. Tena hapatatokea gharika ya kuangamiza nchi." [12] Mungu akasema,
" na hii ndiyo ishara ya agano ambalo ninafanya kati yangu na ninyi pamoja na kila
kiumbe hai kilicho pamoja nanyi, kwa vizazi vyote vya baadaye: [13] Nimeweka upinde
wangu wa mvua katika wingu, na itakuwa ndiyo ishara ya agano kati yangu na nchi.
[14] Hata itakuwa nitakapoleta wingu juu ya nchi na upinde wa mvua ukaonekana
katika wingu, [15] ndipo nitakumbuka agano langu, ambalo ni kati yangu na ninyi na
kila kiumbe hai cha wote mwenye mwili. Maji hayatafanyika tena gharika kuharibu
wote wenye mwili. [16] Upinde wa mvua utakuwa katika mawingu na nitauona, ili
kukumbuka agano la milele kati ya Mungu na kila kiumbe hai cha wote wenye mwili
ambacho kiko juu ya nchi." [17] Kisha Mungu akamwambia Nuhu, " Hii ni ishara ya
agano ambalo nimelithibitisha kati yangu na wenye mwili wote ambao wako juu ya
nchi." [18] Wana wa Nuhu ambao walitoka katika safina walikuwa ni Shemu, Hamu,
na Yafethi. Na Hamu akamzaa kanaani. [19] Watatu hawa walikuwa ndio wana wa
Nuhu, na kutokea kwa hawa nchi yote ikajaa watu. [20] Nuhu akaanza kuwa mkulima,
na akapanda mizabibu. [21] Akanywa sehemu ya divai na akalewa. Akawa amelala
hemeani uchi. [22] Kisha Hamu, baba yake na Kanaani, akaona uchi wa baba yake
na akawaambia ndugu zake wawili waliokuwa nje. [23] Kwa hiyo Shemu na Yafethi
wakachukua kanzu wakaitanda juu ya mabega yao, na wakatembea kinyumenyume
na wakaufunika uchi wa baba yao. Nyuso zao zikiwa zimegeuka nyuma upande
mwingine, kwa hiyo hawakuona uchi wa baba yao. [24] Nuhu alipozinduka kutoka
katika ulevi wake, alijua ni jambo gani mtoto wake mdogo amemfanyia. [25] Hivyo
akasema, "Alaaniwe Kanaani. Na awe mtumishi kwa watumishi wa ndugu zake."
[26] Akasema pia, Yahwe, Mungu wa Shemu, abarikiwe, Kanaani na awe mtumwa wake.
[27] Mungu na apanuwe mipaka ya Yafethi, na afanye makazi yake katika hema za
Shemu. Kanaani na awe mtumwa wake." [28] Baada ya gharika, Nuhu aliishi miaka
miatatu na hamsini. [29] Siku zote za Nuhu zilikuwa ni miaka mia tisa na hamsini, na
kisha alikufa.

# 10

[1] Hivi ndivyo vilikuwa vizazi vya wana wa Nuhu, ambao ni, Shemu, Hamu, na
Yafethi. Wana wa kiume walizaliwa kwao baada ya gharika. [2] Wana wa Yafethi
walikuwa Gomeri, Magogu, Madai, Yavani, Tubali, Masheki, na Tirasi. [3] Na wana wa
Gomeri walikuwa Ashikenazi, Rifathi na Togama. [4] Wana wa Yavani walikuwa Elisha,
Tarshishi, Kitimu, na Dodanimu. [5] Kutoka kwa hawa watu wa pwani waligawanyika
na kwenda kwenye ardhi zao, kila mtu na lugha yake, kufuatana na koo zao, kwa
mataifa yao. [6] Wana wa Hamu walikuwa Kushi, Misraimu, Putu, na Kanaani. [7] Wana
wa Kushi walikuwa Seba, Havila, Sabta, Raama, na Sabteka. Wana wa Raama
walikuwa Sheba na Dedani. [8] Kushi akamzaa Nimrodi, ambaye alikuwa hodari
wa kwanza juu ya nchi. [9] Alikuwa mwindaji mkuu mbele ya Yahwe. Hii ndiyo
sababu hunenwa, "Kama Nimrod mwindaji mkuu mbele za Yahwe." [10] Miji ya
kwanza ya ufalme wake ilikuwa Babeli, Ereku, Akadi na Kalne, katika ichi ya Shinari.
[11] Kutoka katika nchi ile alikwenda Ashuru na akajenga Ninawi, Rehoboth- iri na
Kala, [12] na Raseni ambao ulikuwa kati ya Ninawi na Kala. Ulikuwa mji mkubwa.
[13] Misraimu akazaa Waludi, Waanami, Walehabi, na Wanaftuhi, [14] Wapathrusi na
Wakasluhi ( ambao kwao Wafilisti walitokea), na Wakaftori. [15] Kanaani akamzaa

Sidono, mwanawe wa kwanza, na Hethi, 16 pia na Myebusi, na Mwamori, Mgirgashi,
17 Mhivi, Mwarki, Msini, 18 Mwarvadi, Msemari, na Mhamathi. Baadaye koo za
wakanaani zikasambaa. 19 Mpaka wa Wakanaani ulianzia Sidoni, katika mwelekeo
wa Gerari, hata Gaza, na kama kuelekea Sodoma, Gomora, Adma, na Seboimu hata
Lasha. 20 Hawa walikuwa wana wa Ham, kwa koo zao, kwa lugha zao, katika ardhi
zao na katika mataifa yao. 21 Pia walizaliwa wana kwa Shemu, ndugu yake mkubwa
wa Yafethi. Shemu pia alikuwa baba yao na watu wote wa Eberi. 22 Wana wa Shemu
walikuwa Elamu, Ashuru, Alfaksadi, Ludi, na Aramu. 23 Wana wa Aramu walikuwa
ni Usi, Huli, Getheri, na Mashi. 24 Arfaksadi akamzaa Sela, na Sela akamzaa Eber.
25 Eberi akazaa wana wawili wa kiume. Jina la mmoja aliitwa Pelegi maana katika
siku zake nchi iligawanyika. Jina la ndugu yake aliitwa Yoktani. 26 Yoktani akamzaa
Almodadi, Shelefu, Hasarmawethi, Yera, 27 Hadoram, Uzali, Dikla, 28 Obali, Abimaeli,
Sheba, 29 Ofiri, Havila, na Yobabi. Hawa wote walikuwa wana wa Yoktani. 30 Mpaka
wao ulikuwa unaanzia Mesha, hadi Sefari, mlima wa mashariki. 31 Hawa walikuwa
wana wa Shemu, kulingana na koo zao na lugha zao, katika ardhi zao kulingana na
mataifa yao. 32 Hizi zilikuwa koo za wana wa Nuhu, kulingana na vizazi vyao, kwa
mataifa yao. Kutokea kwa hawa mataifa yaligawanyika na kwenda juu ya nchi baada
ya gharika.

# 11

1 Sasa nchi yote ilikuwa inatumia lugha moja na ilikua na usemi mmoja. 2 Ikawa
waliposafiri upande wa mashariki, wakaona eneo tambarare katika nchi ya Shinari
na wakakaa pale. 3 Wakasemezana, “Haya njoni, tufanye matofari na tuyachome
kikamilifu.” Walikuwa na matofari badala ya mawe na lami kama chokaa.
4 Wakasema, “njoni, na tujenge mji sisi wenyewe na mnara ambao kilele chake
kitafika angani, na tujifanyie jina. Kama hatutafanya, basi tutatawanyika katika uso
wa nchi yote.” 5 Kwa hiyo Yahwe akashuka kuona mji na mnara ambao wazao wa
Ibrahimu walikuwa wamejenga. 6 Yahwe akasema, “Tazama, watu hawa ni taifa moja
na lugha moja, na wameanza kufanya hivi! Hivikaribuni halitashindikana jambo
watakalo kusudia kulifanya. 7 Njoni, tushuke na tuvuruge lugha yao pale, ili kwamba
wasielewane.” 8 Kwa hiyo Yahwe akawatawanya kutoka pale kwenda pande zote
za uso wa nchi na wakaacha kujenga mji. 9 Kwa hiyo, jina lake ukaitwa Babeli, kwa
sababu hapo Yahwe alivuruga lugha ya nchi yote na tangu pale Yahwe akawatawanya
ng'ambo juu ya uso wa nchi yote. 10 Hivi ndivyo vilikuwa vizazi vya Shemu. Shemu
alikuwa na umri wa miaka mia moja, na akamzaa Alfaksadi miaka miwili baada ya
gharika. 11 Shemu akaishi miaka miatano baada ya kumzaa Alfaksadi. Pia akazaa
wana wengine wa kiume na wa kike. 12 Wakati Alfaksadi alipokuwa ameishi miaka
thelathini na mitano akamzaa Shela. 13 Alfaksadi aliishi miaka 403 baada ya kumzaa
Shela. Akawazaa pia wana wengine wa kiume na wa kike. 14 Wakati Shela alipokuwa
ameishi miaka thelathini, akamzaa Eberi. 15 Shela aliishi miaka 403 baada ya kumzaa
Eberi. Akawazaa pia wana wengine wa kiume na wa kike. 16 Wakati Eberi alipokuwa
ameishi miaka thelathini na minne, akamzaa Pelegi. 17 Eberi aliishi miaka 430 baada
ya kumzaa Pelegi. Akawazaa pia wana wengine wa kiume na wa kike. 18 Wakati
Pelegi alipokuwa ameishi miaka thelathini, akamzaa Reu. 19 Pelegi aliishi miaka
209 baada ya kumza a Reu. Akawazaa pia wana wengine wa kiume na wa kike.
20 Wakati Reu alipokuwa ameishi miaka thelathini na miwili, alimzaa Serugi. 21 Reu
aliishi miaka207 baada ya kumzaa Seregu. Akawazaa pia wana wengine wa kiume
na wa kike. 22 Wakati Seregu alipokuwa ameishi miaka thelathini, akamzaa Nahori.
23 Seregu aliishi miaka mia mbili baada ya kumzaa Nahori. Akawazaa pia wana
wengine wa kiume na wa kike. 24 Wakati Nahori alipokuwa ameishi miaka ishirini na

tisa, akamzaa Tera. 25 Nahori aliishi mika 119 baada ya kumzaa Tera. Akawazaa pia
wana wengine wa kiume na wa kike. 26 Baada ya Tera kuishi miaka sabini, akamzaa
Abram, Nahori, na Haran. 27 Hivi ndivyo vilikuwa vizazi vya Tera. Tera alimzaa
Abram, Nahori, na Harani, na Harani akamzaa Lutu. 28 Harani akafa machoni pa
baba yake Tera katika nchi aliyozaliwa, katika Ur wa Wakaldayo. 29 Abram na Nahori
wakajitwalia wake. Mke wa Abram aliitwa Sarai na mke wa Nahori aliitwa Milka,
binti wa Harani, aliyekuwa baba wa Milka na Iska. 30 Sasa Sarai alikuwa Tasa;
hakuwa na mtoto. 31 Tera akamtwaa Abram mwanawe, Lutu mwana wa mwanawe
Harani, na Sarai mkwewe, mke wa mwanawe Abram, na kwa pamoja wakatoka Ur
wa Wakaldayo, kwenda katika nchi ya Kanaani. Lakini walipofika Harani wakakaa
pale. 32 Tera akaishi miaka 205 kisha akafa hapao Harani.

# 12

1 Kisha Yahwe akamwambia Abram, “Nenda utoke katika nchi yako, na toka kwa
ndugu zako, na kwa jamaa za baba yako, uende katika nchi nitakayo kuonesha.
2 Nitakufanya uwe taifa kubwa, na nitakubariki na kulifanya jinalako kuwa kubwa,
na utafanyika baraka. 3 Nitawabariki wakubarikio, lakini asiye kuheshimu nita
mlaani. Kupitia kwako familia zote za nchi zitabarikiwa. 4 Kwa hiyo Abram
akaondoka kama vile Yahwe alivyo mwambia kufanya, na Lutu akaenda pamoja
naye. Abram alikuwa na miaka sabini na mitano wakati alipotoka Harani. 5 Abram
akamchukua Sarai mkewe, Lutu, mtoto wa ndugu yake, na vyote walivyomiliki
ambavyo wamevikusanya, na watu ambao wamewapata wakiwa huko Harani.
Wakatoka kwenda katika nchi ya Kanaani, wakafika nchi ya Kanaani. 6 Abram
akapitia katikati ya nchi hadi Shekemu, hadi mwaloni wa More. Wakati huo
wakanaani waliishi katika nchi hiyo. 7 Yahwe akamtokea Abram, na kusema,
“Nitawapa uzao wako nchi hii.” Kwa hiyo Abram akamjengea madhabahu, Yahwe
ambaye alimtokea. 8 Kutoka pale akaenda kwenye nchi ya mlima mashariki mwa
Betheli, ambapo alipiga hema yake, magaribi kukiwa na Betheli na mashariki kukiwa
na mji wa Ai. Akajenga madhabahu ya Yahwe pale na kuliitia jina la Yahwe. 9 Kisha
Abram akaendelea kusafiri, akielekea upande wa Negebu. 10 Kulikuwa na njaa katika
nchi, kwa hiyo Abram akaenda kukaa Misri, kwa kuwa njaa ilikua kali katika nchi.
11 Wakati alipokaribia kuingia Misri, akamwambia Sarai mkewe, “tazama, najua
kuwa wewe ni mwanamke mzuri. 12 Wamisri watakapokuona watasema, huyu ni
mke wake, na wataniua mimi, lakini watakuacha wewe hai. 13 Hivyo wewe sema
kuwa ni dada yangu, ili kwamba niwe salama kwa sababu yako, na kumba maisha
yangu yatasalimika kwa sababu yako.” 14 Ikawa kwamba Abram alipoingia Misri,
Wamisri wakaona kwamba Sarai ni mzuri sana. 15 Wakuu wa Farao wakamuona, na
kumsifia kwa Farao, na huyu mwanamke akachukuliwa kupelekwa nyumbani mwa
Farao. 16 Farao akamtendea kwa wema Abram kwa ajili yake, na akampatia kondoo,
maksai, punda waume watumishi wa kiume, watumishi wa kike, punda wake, na
ngamia. 17 Kisha Yahwe akampiga Farao na nyumba yake kwa mapigo makuu kwa
sababau ya Sarai, mke wa Abram. 18 Farao akamwita Abram na kusema, “Nini hiki
ambacho umenifanyia? Kwa nini hukuniambia kuwa alikuwa mke wako? 19 Kwa
nini ulisema, 'ni dada yangu; na mimi nikamchukua kuwa mke wangu? Sasa kwa
sababu hiyo huyu hapa mke wako. Mchukue na uende zako.” 20 Kisha Farao akatoa
amri kwa watu wake kuhusiana naye, na wakamuondoa, yeye pamoja na mke wake
na vyote alivyokuwa navyo.

# 13

1 Kwa hiyo Abram akaondoka akatoka Misri na akaenda Negebu, Yeye, mke wake,

na vyote alivyokuwa navyo. Lutu pia akaenda pamoja naye. 2 Na sasa Abram alikuwa
tajiri wa mifugo, fedha na dhahabu. 3 Aliendelea na safari yake kutoka Negebu hadi
Betheli, mahali ambapo hema yake ilikuwa tangu mwanzo, kati ya Betheli na mji
wa Ai. 4 Akaenda mahali ambapo madhabahu ilikuwa imejengwa mwanzoni. Hapa
akaliitia jina la Yahwe. 5 aliyekuwa anasafiri na Abram, alikuwa pia na ngo'mbe,
makundi ya mifugo, na mahema. 6 Nchi haikuwatosha wote kukaa pamoja karibu
kwa sababu mali zao zilikuwa nyingi sana, kiasi kwamba hawakuweza kukaa pamoja.
7 Pia, kulikuwa na ugomvi kati ya wachunga wanyama wa Abram na wachunga
wanyama wa Lutu. Wakanaani pamoja na Waperizi walikuwa wakiishi katika nchi
ile wakati huo. 8 Kwa hiyo Abram akamwambia Lutu, "Pasiwe na ugomvi kati yako
na mimi, na kati ya wachunga wanyama wako na wachunga wanyama wangu; licha
ya hayo sisi ni familia. 9 Je nchi hii yote haiko mbele yako? Nenda na ujitenge
na mi. Ikiwa utakwenda kushoto, mimi nitakwenda kulia. au ikiwa utakwenda
kulia, mimi nitakwenda kushoto." 10 Kwa hiyo Lutu akatazama, na akaona kuwa
nchi yote tambarare ya Yorodani ilikuwa na maji kila mahali hadi Zoari, kama vile
bustani ya Yahwe, na kama nchi ya Misri. Hii ilikuwa ni kabla Yahwe hajaiangamiza
Sodoma na Gomora. 11 Kwa hiyo Lutu akajichagulia yeye mwenyewe nchi tambarare
ya Yorodani na akasafiri mashariki, na ndugu hawa wakatengana wao kwa wao.
12 Abram akaishi katika nchi ya Kanaani, na Lutu akaishi katika miji ya tambarare.
Akatandaza hema zake hadi Sodoma. 13 Na sasa watu wa Sodoma walikuwa waovu
na wenye dhambi nyingi dhidi ya Yahwe. 14 Yahwe akamwambia Abram baada ya
Lutu kuondoka kwake, "Angalia kuanzia mahali ulipo simama hadi kaskazini, kusini,
mashariki, na magharibi. 15 Nchi yote hii uionayo, nitakupatia wewe pamoja na
uzao wako milele. 16 Nitawafanya uzao wako kuwa wengi kama mavumbi ya nchi,
kiasi kwamba kama kuna mtu anaweza kuhesabu mavumbi ya nchi, ndipo na uzao
wako pia utahesabika. 17 Inuka, tembea katika urefu na upana wa nchi hii, kwa
kuwa nitakupatia." 18 Kwa hiyo Abram akachukua hema yake, akaja na kukaa katika
mwaloni wa Mamre, ambao uko Hebroni, na pale akajenga Madhabahu ya Yahwe.

# 14

1 Ikiwa katika siku za Amrafeli, mfalme wa shinari, Arioko, mfalme wa Elasari,
Kedorlaoma, mfalme wa Elam na Tidali, mfalme wa Goimu, 2 walifanya vita dhidi ya
Bera mfalme wa Sodoma, Birsha, mfalme wa Gomora, Shinabu, mfalme wa Adma,
Shemeberi, mfalme wa Seboim, na mfalme wa Bela(pia ikiitwa Soari). 3 Hawa
wafalme watano wa mwisho waliungana pamoja katika bonde la Sidim (pia likiitwa
bahari ya chumvi). 4 Kwa miaka kumi na mbili walimtumikia Kedorlaoma, lakini
katika mwaka wa kumi na tatu waliasi. 5 Kisha katika mwaka wa kumi na
nne, Kedorlaoma na wafalme waliokuwa pamoja nae walikuja na kuwashambulia
Warefai katika Ashteroth Karnaimu, na Wazuzi katika Hamu, Waemi katika Shawe
Kiriathaimu, 6 na Wahori katika mlima wao wa Seiri, mpaka El Parani iliyo karibu na
jangwa. 7 Kisha wakarudi wakaja En Misifati (Pia ikiitwa Kadeshi), na kuishinda nchi
yote ya Waamaleki, na pia Waamori ambao waliishi Hasasoni Tamari. 8 Kisha mfalme
wa Sodoma, mfalme wa Gomora, mfalme wa Adma, mfalme wa Seboim, na mfalme
wa Bela (pia ikiitwa Soari) walikwenda na kuandaa vita 9 dhidi ya Kadorlaoma,
mfalme wa Elam, Tidali mfalme wa Goim, Amrafeli, mfalme wa Shinari, Arioki,
mfalme wa Elasari; wafme wanne dhidi ya wale watano. 10 Na sasa bonde la Sidimu
lilikuwa limejaa mashimo ya lami, na wafalme wa Sodoma na Gomora walipokimbia,
wakaanguka pale. Wale waliosalia wakakimbilia milimani. 11 Kwa hiyo adui
akachukua mali zote za Sodoma na Gomora na vyakula vyao vyote, na wakaenda
zao, 12 walipoondoka, wakamchukua pia Lutu, mtoto wa ndugu yake na Abram
ambaye aliishi Sodoma, pamoja na mali zake zote. 13 Mmoja ambaye alitoroka alikuja

na kumwambia Abram mwebrania. Alikuwa anaishi katika mialoni ya Mamre,
mwamori ambaye alikuwa ni ndugu wa Eshkoli na Aneri ambao walikuwa washirika
wa Abram. 14 Abram aliposikia kuwa maadui wamemteka ndugu yake, akawaongoza
wanaume waliofunzwa na kuzaliwa nyumbani mwake 318 na akawaongoza hadi
Dani. 15 Akawagawanya watu wake dhidi yao usiku na kuwavamia, na kuwafukuza
mpaka Hoba, ambayo iko kaskazini mwa Dameski. 16 Kisha akarudisha mali zote, pia
akamrudisha ndugu yake Lutu na mali zake, pamoja na wanawake na watu wengine.
17 Baada ya Abram kurudi kutoka kumpiga Kadorlaoma na wafalme waliokuwa
pamoja nae, mfalme wa Sodoma akatoka kuonana nae katika bonde la Shawe (pia
iliitwa bonde la mfalme). 18 Melkizedeki, mfalme wa Salem, akaleta mkate na divai.
Alikuwa ni kuhani wa Mungu aliye juu sana. 19 Alimbariki akisema, “Abarikiwea
Abram na Mungu aliye juu sana, muumba wa mbingu na nchi. 20 Abarikiwe Mungu
aliye juu sana, ambaye amekupatia adui zako katika mikono yako.” Kisha Abram
akampatia sehemu ya kumi ya kila kitu. 21 Mfalme wa Sodama akamwambia Abram,
“Nipatie watu, na ujichukulie wewe mwenyewe mali.” 22 Abram akamwambia
mfalme wa Sodoma, “Nimeinua juu mkono wangu kwa Yahwe, Mungu aliye juu sana,
muumbaji wa mbingu na nchi, 23 kwamba sitachukua uzi wala gidamu ya kiatu, au
kitu chochote ambacho ni chako, 'ili kwamba usiseme, nimemfanya Abram kuwa
tajiri.' 24 Sitachukua chochote isipokuwa kile ambacho vijana wamekula na sehemu
za watu waliokwenda nami. Aneri, Eskoli, na Mamre na wachukue sehemu zao.”

# 15

1 Baada ya mabo haya neno la Yahwe likamjia Abram katika maono, likisema,
“Usiogope, Abram! mimi ni ngao yako na thawabu yako kubwa sana.” 2 Abram
akasema, “Bwana Yahwe, utanipatia nini, kwa kuwa naenda bila mtoto, na mrithi wa
nyumba yangu ni Eliezeri wa Dameski?” 3 Abram akasema, “Kwakuwa hujanipatia
uzao, tazama, mwangalizi wa nyumba yangu ndiye mrithi wangu.” 4 Kisha, tazama,
neno la Yahwe likaja kwake, kusema, “Mtu huyu hatakuwa mrithi wako; isipokuwa
atakaye toka katika mwili wako ndiye atakuwa mrithi wako.” 5 Kisha akamtoa nje, na
akasema, Tazama mbinguni, na uzihesabu nyota, ikiwa unaweza kuzihesabu.” Kisha
akamwambia, hivyo ndivyo uzao wako utakavyokuwa. 6 Akamwamini Yahwe, na
akamuhesabia jambo hili kuwa mwenye haki. 7 Akamwambia, Mimi ni Yahwe, niliye
kutoa katika Uru ya Wakaldayo, na kukupatia nchi hii kuirithi.” 8 Akasema, “Bwana
Yahwe, nitajua je kuwa nitairithi?” 9 Kisha akamwambia, “Nipatie ndama wa umri wa
miaka mitatu, mbuzi mke wa umri wa miaka mitatu, na kondoo mume wa umri wa
miaka mitatu, na njiwa na mwana njiwa.” 10 Akamletea hivi vyote, akavipasua katika
sehemu mbili, akaweka kila kipande kuelekea mwenzake, ila ndege hakuawapasua.
11 Wakati ndege walipokuja juu ya mizoga, Abram akawafukuza. 12 Kisha wakati
jua lilipokuwa likizama, Abram akalala usingizi mzito na tazama, hofu ya giza kuu
ikamfunika. 13 Kisha Yahwe akamwambia Abram, “Ujuwe kwa hakika kwamba uzao
wako watakuwa wageni katika nchi ambayo si ya kwao, na watatumikishwa na
kuteswa kwa miaka mia nne. 14 Nitahukumu taifa ambalo watalitumikia, na baadye
watatoka wakiwa na mali nyingi. 15 Lakini utakwenda kwa baba zako kwa amani,
na utazikwa katika uzee mwema. 16 Katika kizazi cha nne watakuja tena hapa, kwa
sababu uovu wa Waamori haujafikia mwisho wake.” 17 Jua lilipokuwa limezama na
kuwa giza, tazama, chungu cha moshi wenye moto na miali ya mwanga ilipita kati ya
vile vipande. 18 Siku hiyo Yahwe akafanya agano na Abram, akisema, “Ninatoa nchi
hii kwa uzao wako, kutoka mto wa Misri hadi kwenye mto mkuu, Frati - 19 Mkeni,
Mkenizi, na Mkadmoni, 20 Mhiti, Mperizi, Mrefai, 21 Mwamori, Mkanaani, Mgirgashi,
na Myebusi.

# 16

1 Kisha Sarai mke wa Abram, alikuwa hajamzalia mtoto, lakini alikuwa na mtumishi
wa kike, Mmisri ambaye jina lake aliitwa Hajiri. 2 Kwa hiyo Sarai akamwambia
Abram, “Tazama, Yahwe hajanifanya mimi kuwa na watoto. Nenda na ulale na
mtumishi wangu. Ili kwamba niweze kupata watoto kupitia yeye.” Abram akasikiliza
sauti ya Sarai. 3 Ilikuwa baada ya Abram kuishi miaka kumi katika nchi ya Kanaani
ndipo Sarai, mke wa Abram, alimtoa Hajiri yule mmisri mtumishi wake kwa mume
wake awe kama mke wake. 4 Kwa hiyo akawa na mahusiano na Hajiri, na akabeba
mimba. Na alipoona kuwa amebeba mimba, akamdharau bibi yake. 5 Kisha Sarai
akamwambia Abram, “Jambo hili baya kwangu ni kwa sababu yako. Nilimtoa
mtumishi wangu wa kike katika kumbatio lako. Na alipoona kuwa amebeba mimba,
nilidharaulika machoni pake. Na sasa acha Yahwe aamuwe kati yangu na wewe.”
6 Lakini Abram akamwambia Sarai, “Tazama, hapa, mtumishi wako yuko katika
uwezo wako, fanya unachofikiri ni kizuri sana kwake.” Kwa hiyo Sarai akakabiliana
naye kwa ukatili, na akatoroka. 7 Malaika wa Yahwe akamkuta karibu na chemichemi
ya maji katika jangwa, chemichemi iliyo katika njia kuelekea Shuri. 8 Akasema,
Hajiri, mtumishi wa Sarai, umetoka wapi na unakwenda wapi?” Na akasema,
ninamtoroka bibi yangu Sarai.” 9 Malaika wa Yahwe akamwambia, “ Rudi kwa
bibi yako, na unyenyekee chini ya mamlaka yake.” 10 Kisha Malaika wa Yahwe
akamwambia, “Nitazidisha uzao wako maradufu, kiasi kwamba watakuwa wengi
wasioweza kuhesabika.” 11 Malaika wa Yahwe pia akamwambia, “ Tazama, wewe
unamimba, na utazaa mtoto kiume, na utamwita jina lake Ishmaeli, kwasabab Yahwe
amesikia mateso yako. 12 Atakuwa punda mwitu wa mtu. Atakuwa adui dhidi ya kila
mtu, na kila mtu atakuwa adui yake, na ataishi kando na ndugu zake wote.” 13 Kisha
akamwita jina hili Yahwe aliye zungumza naye, “Wewe ni Mungu unionaye mimi,”
kwa kuwa alisema, “je ninaendelea kweli kuona, hata baada ya kuwa ameniona?”
14 Kwa hiyo kisima kiliitwa Beerlahairori; Tazama, kiko kati ya Kadeshi na Beredi.
15 Hajiri akamzalia Abram mwana wa kiume, na Abram akamwita mwanawe, ambaye
Hajiri amemzaa jina, Ishmaeli. 16 Abram alikuwa na umri wa miaka themanini na
sita wakati Hajiri alipomzaa Ishmaeli kwa Abram.

# 17

1 Wakati Abram alipokuwa na umri wa miaka tisini na tisa, Yahwe alimtokea Abram
na akamwambia, “Mimi ni Mungu wa uwezo. Uende mbele yangu, na uwe mkamilifu.
2 Kisha nitalithibitisha agano langu kati yangu mimi na wewe, na nitakuzidisha
sana. 3 Abram akainama uso wake hadi chini ardhini na Mungu akazungumza
naye, akisema, 4 “Mimi, tazama, agano langu liko nawe. Utakuwa baba wa mataifa
mengi. 5 Wala jina lako halitakuwa tena Abram, bali jina lako litakuwa Abraham -
kwa kuwa ninakuchagua kuwa baba wa mataifa mengi. 6 Nitakufanya uwe na uzao
mwingi zaidi, na nitakufanya mataifa, na wafalme watatoka kwako. 7 Nitaimarisha
agao langu kati yangu mimi na wewe na uzao wako baada yako, katika vizazi vyao
vyote kwa agano la milele, nitakuwa Mungu kwako na kwa wazao wako baada yako.
8 Nitakupa wewe, na wazao wako baada yako, nchi ambayo ulikuwa unaishi, nchi
yote ya Kanaani, kuwa miliki ya milele, na nitakuwa Mungu wao.” 9 Kisha Mungu
akamwambia Abraham, “nawe lazima ulishike agano langu, wewe pamoja na uzao
wako baada yako kwa vizazi vyao. 10 Hili ndilo agano langu, ambalo utalishika, kati
yangu na wewe na wazao wako baada yako: Kila mwanaume wa kwenu lazima
atahiriwe. 11 Lazima mtatahiriwa katika nyama ya govi la ngozi ya mbele, na hii
itakuwa ishara ya agano kati yangu mimi na ninyi. 12 Kila mwanaume wa kwenu
aliye na umri wa siku nane lazima atahiriwe, katika vizazi ya watu wenu. Hii

ni pamoja na yule azaliwaye katika nyumba yako na yeye ambaye amenunuliwa
kwa fedha kutoka kwa mgeni yeyote ambaye si mmoja wa wazao wako. 13 Mtu
ambaye amezaliwa katika nyumba yako na yule aliye nunuliwa kwa fedha yako
lazima atahiriwe. Hivyo agano langu litakuwa katika mwili wenu kuwa agano la
milele. 14 Mwanaume yeyote asiye tahiriwa katika mwili govi la ngozi yake ya mbele
atatengwa na watu wake. Amevunja agano langu.” 15 Mungu akamwambia Abraham,
“kwa habari ya Sarai mkeo, usimuite tena Sarai. Badala yake jina lake litakuwa Sara.
16 Nitambariki, na nitakupatia mtoto wa kiume kwake. Nitambariki, na atakuwa
mama wa mataifa. Wafalme wa watu wa mataifa watapatikana kutokana na yeye.
17 Kisha Abraham akainama uso wake hadi ardhini, na akacheka, akasema moyoni
mwake, Je yawezekana mtoto azaliwe kwa mwanaume ambaye ana umri wa miaka
miamoja? na Je Sara, ambaye ana umri wa miaka tisini anaweza kuzaa mwana?”
18 Abraham akamwambia Mungu, “Lau Ishmaeli angeweza kuishi kabla yako!”
19 Mungu akasema, Hapana, Sarai mkeo atakuzalia mtoto wa kiume na utamwita
jina lake Isaka. Nita imarisha agano langu na yeye kama agano la milele pamoja
na uzao wake baada yake. 20 Na kwa habari ya Ishmaeli nimekusikia. Tazama,
ninambariki, na nitamfanya kuwa na uzao na kumzidisha maradufu. Atakuwa
baba wa viongozi kumi na mbili wa makabila, na nitamfanya kuwa taifa kuu.
21 Lakini agano langu nitalifanya imara na Isaka, ambaye Sarai atazaa kwako majira
haya mwakani.” 22 Alipo kuwa amemaliza kuzungumza naye, Mungu akaondoka
kwa Abraham. 23 Kisha Abraham akamtwaa Ishmaeli mwanawe, na wote ambao
walizaliwa katika nyumba yake, na wote ambao walinunuliwa kwa fedha yake, kila
mwanaume miongoni mwa watu wa nyumba ya Abraham, walitahiriwa mwili wa
magovi ya ngozi ya mbele katika siku iyo hiyo, kama Mungu alivyo kuwa amesema.
24 Abraham alikuwa na umri wa miaka tisini na tisa alipotahiriwa katika mwili
wa govi la ngozi yake ya mbele. 25 Na Ishmaeli mwanawe alikuwa na umri wa
miaka kumi na tatu alipotahiriwa katika mwili wa govi la ngozi yake ya mbele.
26 Siku ile ile ambayo wote wawili Abraham na Ishmael mwanawe walipotahiriwa,
ndipo 27 wanaume wote wa nyumba yake walitahiriwa pia, hawa ni pamoja na wale
waliozaliwa katika nyumba ile na wale walionunuliwa kwa fedha kutoka kwa mgeni.

# 18

1 Yahwe alimtokea Abraham katika Mialoni ya Mamre, alipokua ameketi mlangoni
pa hema wakati wa jua. 2 Akatazama juu na, tazama, akaona wanaume watatu
wamesimama mbele yake. Alipo waona, alikimbia kupitia mlango wa hema kuwalaki
na kuinama chini hadi ardhini. 3 Akasema, “Bwana, kama nimepata upendelea
machoni pako, nakuomba usinipite na kuniacha mtumishi wako. 4 Naomba maji
kidogo yaletwe, mnawe miguu yenu, na mjipumzishe chini ya mti. 5 Nami acha
nilete chakula kidogo, ili kwamba mjiburudishe wenyewe. Ndipo baadae mwaweza
kwenda zenu, kwa kuwa mmekuja kwa mtumishi wenu.” Nao wakasema, “Fanya
kama ulivyo sema.” 6 Kisha Abraham akaenda upesi hemani kwa Sara, na akasema,
“Harakisha, chukua vipimo vitatu vya unga safi, uukande, na fanya mkate.” 7 Kisha
Abraham akakimbia kundini, akachukua ndama wa ng'ombe aliye laini na mzuri,
na akampatia mtumishi na kwa haraka akamwandaa. 8 Akatwaa siagi na maziwa
na ndama aliye kwisha andaliwa, na akaweka chakula mbele yao, naye akasimama
karibu nao chini ya mti wakati wanakula. 9 Wakamwambia, “Mke wako Sara
yuko wapi?” akajibu. “pale hemani.” 10 akasema, “Hakika nitarejea kwako
majira ya machipuko, na tazama Sara mkeo atakuwa na mtoto wa kiume.” Sara
alikuwa akisikiliza mlangoni pa hema iliyokuwa nyuma yake. 11 Abraham na Sara
walikuwa wazee, umri wao ulikuwa umeendelea sana, na Sara alikuwa amepita umri

ambao mwanamke anaweza kuzaa watoto. [12] Kwa hiyo Sara akajicheka mwenyewe,
akijisemesha mwenyewe, “baada ya kuwa nimechakaa na bwana wangu ni mzee, je
ni tapata furaha hii?” [13] Yahwe akamwambia Abraham, “Kwa nini Sara amecheka na
kusema, Je ni kweli nitazaa mtoto, nikiwa mzee'? [14] Je kuna jambo lolote gumu sana
kwa Yahwe? Itakuwa katika wakati nilioweka mimi majira ya machipuko, nitarejea
kwako. Majira haya mwakani Sara atakuwa na mtoto wa kiume.” [15] Kisha Sara
akakataa na kusema, “sikucheka,” kwa kuwa aliogopa. Yahwe akasema, “hapana
ulicheka.” [16] Kisha wale wanaume walisimama kuondoka na wakatazama chini
kuelekea Sodoma. Abraham akafuatana nao kuona njia yao. [17] Lakini Yahwe
akasema, Je ni mfiche Abraham kile ninacho kusudia kufanya, [18] Ikiwa kwa hakika
Abraham atakuwa mkuu na taifa lenye nguvu, na katika yeye mataifa yote ya dunia
watabarikiwa? [19] Kwa kuwa nimemchagua ili awaelekeze wanawe na nyumba yake
baada yake waishike njia ya Yahwe, watende utakatifu na haki, ili kwamba Yahwe
ampatie Abraham yale aliyo yasema kwake.” [20] Kisha Yahwe akasema, “Kwa sababu
kilio cha Sodoma na Gomora ni kikuu, na kwa kuwa dhambi yao ni kubwa, [21] sasa
nitashuka pale na kuona kilio kilicho nifikia dhidi yake, ikiwa kweli wamefanya
au hawakufanya, nitajua.” [22] Kwa hiyo wale wanaume wakageuka toka pale, na
kuelekea Sodoma, lakini Abraham akabaki amesimama mbele ya Yahwe. [23] Kisha
Abraham alikaribia na kusema, “Je utawafutilia mbali watakatifu pamoja na waovu?
[24] Huenda wakawepo wenye haki hamsini katika mji. Je utawakatilia mbali na
usiuache mji kwa ajili ya hao watakatifu hamsini walioko hapo? [25] Hasha usifanye
hivyo, kuwauwa watakatifu pamoja na waovu, ili kwamba watakatifu watendewe
sawa na waovu. Hasha! Je muhukumu wa ulimwengu wote hatatenda haki?”
[26] Yahwe akasema, “Katika Sodoma nikipata watakatifu hamsini kwenye mji, nita
uacha mji wote kwa ajili ya hao.” [27] Abraham akajibu na kusema, “Tazama,
Nimeshika kusema na Bwana wangu, hata kama mimi ni mavumbi na majivu!
[28] Itakuwaje ikiwa kuna watano pungufu katika idadi ya hao watakatifu hamsini?
Je utaangamiza mji wote kwa upungufu wa hao watano?” Akasema, “Sitaangamiza,
ikiwa nitapata watu arobaini na watano pale.” [29] Akaongea naye tena, na kusema,
“Itakuwaje ikiwa arobaini watapatikana pale?” Akajibu, “Sitafanya kwa ajili ya hao
arobaini.” [30] Akasema, Tafadhali usikasirike, Bwana, nikiongea. Pengine thelathini
watapatikana pale.” Akajibu, 'Sitafanya, ikiwa nitapata thelathini pale.” [31] Akasema,
Tazama, Nimeshika kusema na Bwana wangu! Pengine ishirini watapatikana pale.”
Akajibu, “Sitaharibu kwa ajili ya hao ishirini.” [32] Akasema, “Tafadhali usikasirike,
Bwana, na nitasema jambo hili kwa mara ya mwisho. Huenda kumi wakaonekana
kule.” Na akasema, sitaangamiza kwa ajili ya hao kumi.” [33] Yahwe akaendelea na
njia yake mara tu baada ya kumaliza kuongea na Abraham, na Abraham akarudi
nyumbani.

# 19

[1] Malaika wawili wakaja Sodoma jioni, wakati ambao Lutu alikuwa amekaa langoni
mwa Sodoma. Lutu akawaona, akainuka kuwalaki, na akainama uso wake chini
ardhini. [2] Akasema, Tafadhari Bwana zangu, nawasihi mgeuke mwende kwenye
nyumba ya mtumishi wenu, mlale pale usiku na muoshe miguu yenu. Kisha
muamke asubuhi na mapema muondoke.” Nao wakasema, “Hapana, usiku tutalala
mjini.” [3] Lakini akawasihi sana, mwishowe wakaondoka pamoja nae, na wakaingia
katika nyumba yake. Akaandaa chakula na kuoka mkate usiotiwa chachu, wakala.
[4] Lakini kabla hawaja lala, wanaume wa mji, wa Sodoma, vijana kwa wazee
wakaizunguka nyumba, wanaume wote kutoka kila kona ya mji. [5] Wakamwita
Lutu, na kumwambia, “Wale wanaume walioingia kwako usiku wakowapi? watoe

hapa nje waje kwetu, ili tuweze kulala nao." 6 Lutu akatoka nje na akafunga
mlango. 7 Akasema, "Nawasihi, ndugu zangu, msitende uovu. 8 Tazama, nina mabinti
wawili ambao hawajawahi kulala na mwanaume yeyote. Nawaomba tafadhari
niwalete kwenu, na muwafanyie lolote muonalo kuwa jema machoni penu. Msitende
lolote kwa wanaume hawa, kwa kuwa wamekuja chini ya kivuli cha dari yangu."
9 Wakasema, "Ondoka hapa!" Wakasema pia, huyu alikuja kukaa hapa kama mgeni,
na sasa amekuwa mwamuzi! Sasa tutakushugulilia vibaya wewe kuliko wao."
Wakamsonga sana huyo mtu, huyo Lutu, na wakakaribia kuvunja mlango. 10 Lakini
wale wanaume wakamkamata Lutu na kumweka ndani na wakafunga mlango.
11 Kisha wale wageni wa Lutu wakawapiga kwa upofu wale wanaume waliokuwa
nje ya nyumba, vijana na wazee kwa pamoja, kiasi kwamba wakachoka wakati
wakiutafuta mlango. 12 Basi wale watu wakamwambia Lutu, Je una mtu mwingine
yeyote hapa? wakwe zako, wanao na mabinti zako, na yeyote mwingine katika
huu mji, ukawatoe hapa. 13 Kwa kuwa tunakaribia kuiangamiza sehemu hii, kwa
sababu mashitaka dhidi yake mbele ya Yahwe yamezidi kiasi kwamba ametutuma
kuuangamiza." 14 Lutu akatoka na akazungumza na wakwe zake, wanaume ambao
walikuwa wamewaposa binti zake, akawambia, "Ondokeni upesi mahali hapa, kwa
kuwa Yahwe anakaribia kuuangamiza mji." Lakini kwa wakwe zake alionekana
kuwa anawatania. 15 Alfajiri, malaika wakamsihi Lutu, wakisema, ondoka, mtwae
mkeo na binti zako wawili ambao wako hapa, ili kwamba usipotelee katika adhabu
ya mji huu." 16 Lakini akakawia-kawia. Kwa hiyo watu wale wakamshika mkono
wake, na mkono wa mkewe, na mikono ya binti zake wawili, kwa sababu Yahwe
alimhurumia. Wakawatoa nje, na kuwaweka nje ya mji. 17 Wakisha kuwatoa
nje mmoja wa wale watu akasema, "jiponye nafsi yako! usitazame nyuma, au
usikae mahali popote kwenye hili bonde. Toroka uende milimani ili kwamba
usije ukatoweshwa mbali." 18 Lutu akawambia, "Hapana, tafadhali bwana zangu!
19 Mtumishi wenu amepata kibali machoni pako, na umenionesha wema ulio mkuu
kwa kuokoa maisha yangu, lakini sitaweza kutorokea milimani, kwa sababu mabaya
yataniwahi na nitakufa. 20 Tazama, ule mji pale uko karibu nijisalimishe pale, na
ni mdogo. Tafadhari niacheni nikimbilie pale ( Je Siyo mdogo ule?), na maisha
yangu yataokolewa." 21 Akamwambia, "Sawa, nimekubali ombi hili pia, kwamba
sitaangamiza mji ambaoumeutaja. 22 Harakisha! toroka uende pale, kwa kuwa
sitafanya chochote mpaka ufike pale." kwa hiyo mji ule ukaitwa Soari. 23 Jua
lilikuwa limekwisha chomoza juu ya nchi wakati Lutu alipofika Soari. 24 Kisha
Yahwe akanyesha juu ya Sodoma na Gomora kiberiti na moto toka kwa Yahwe
mbinguni. 25 Akaharibu miji ile, na bonde lote, na vyote vilivyomo katika miji, na
mimea iliyo chipua juu ya ardhi. 26 Lakini mke wa Lutu aliye kuwa nyuma yake,
akatazama nyuma, na akawa nguzo ya chumvi. 27 Abraham akaamuka asubuhi na
mapema akaenda mahali alipokuwa amesimama mbele ya Yahwe. 28 Akatazama
chini kuelekea Sodoma na Gomora na kuelekea katika nchi yote bondeni. Akaona
na tazama, moshi ulikuwauki ukienda juu kutoka chini kama moshi wa tanuru.
29 Wakati Mungu alipoharibu miji ya bondeni, Mungu akamkumbuka Abraham.
Akamtoa Lutu kutoka katika maangamizi alipoangamiza miji ambayo katika hiyo
Lutu aliishi. 30 Lakini Lutu akapanda juu kutoka Soari na kwenda kuishi katika
milima akiwa pamoja na binti zake wawili, kwa sababu aliogopa kuishi Soari. Kwa
hiyo akaishi pangoni, yeye na binti zake wawili. 31 Yule wa kwanza akamwambia
yule mdogo, "Baba yetu ni mzee, na hakuna mwanaume mahali popote wa kulala na
sisi kulingana na desturi ya dunia yote. 32 Njoo na tumnyweshe baba yetu mvinyo na
tulale naye ili kwamba tuendeleze uzao wa baba yetu." 33 Kwa hiyo wakamnywesha
baba yako mvinyo usiku ule. Kisha yule wa kwanza akaingia na akalala na baba yake;

Baba yake hakujua ni wakati gani alikuja kulala, wala wakati alipo amka. 34 Siku iliyo
fuata yule wa kwanza akamwambia mdogowake, “Sikiliza, usiku wa jana nililala
na baba yangu. Na tumnyweshe mvinyo usiku wa leo pia, na uingie ukalale naye.
Ili kwamba tuendeleze uzao wa baba yetu.” 35 Kwa hiyo wakamnywesha baba yao
mvinyo usiku ule pia, na yule mdogo akaenda na akalala naye. Baba yake hakujua
ni wakati gani alilala, wala wakati alipoamka. 36 Basi hao binti wote wawili wa
Lutu wakapata mimba kwa baba yao. 37 Wa kwanza akazaa mwana wa kiume, na
akamwita jina lake Moabu. Akawa ndiye baba wa wamoabu hata leo. 38 Nayule
mdogo naye akazaa mwana wa kiume, na akamwita Benami. Huyu ndiye baba wa
watu wa Waamoni hata leo.

# 20

1 Abraham akasafiri kutoka pale hadi nchi ya Negebu, na akakaa kati ya Kadeshi
na Shuri. Akawa mgeni akiishi Gerari. 2 Abraham akasema kususu mkewe Sara, “ni
dada yangu.” Kwa hiyo Abimeleki mfalme wa Gerari akatuma watu wake kumchukua
Sara. 3 Lakini Mungu akamtokea Abimeleki usiku katika ndoto, akamwambia,
“Tazama, wewe ni mfu kutokana na mwanamke uliye mchukua, kwa kuwa ni mke wa
mtu.” 4 Basi Abimeleki alikuwa bado hajamkaribia hivyo akasema, “Bwana, Je utaua
hata taifa lenye haki? 5 Je si yeye mwenyewe aliye niambia, 'Sara ni dada yangu?'
Hata Sara mwenyewe alisema, 'ni kaka yangu.' Nimefanya hili katika uadilifu wa
moyo wangu na katika mikono isiyo na hatia.” 6 Kisha Mungu akasema naye katika
ndoto, “Kweli, ninajua pia kwamba umefanya hili katika uadilifu wa moyo wako, na
pia nilikuzuia usitende dhambi dhidi yangu mimi. Ndiyo maana sikuruhusu umshike.
7 Kwa hiyo, mrudishe huyo mke wa mtu, kwa kuwa ni nabii. Atakuombea, na utaishi.
Lakini usipo mrudisha, ujuwe kwamba wewe pamoja na wote walio wa kwako
mtakufa hakika. 8 Abimeleki akaamka asubuhi na mapema akawaita watumishi
wake wote waje kwake. Akawasimulia mambo haya yote, na watu wale wakaogopa
sana. 9 Kisha Abimeleki akamwita Abraham na kumwambia, “Umetufanyia jambo
gani? Ni kwa jinsi gani nimekutenda dhambi kwamba umeniletea mimi na ufalme
wangu dhambi hii kubwa? Umenifanyia mimi jambo ambalo halipaswi kufanywa.”
10 Abimeleki akamwambia Abraham, “Nini kilikushawishi wewe kutenda jambo
hili?” 11 Abraham akasema, “Ni kwasababu nilifikiri hakika hakuna hofu ya Mungu
katika sehemu hii, na kwamba wataniua kwa ajili ya mke wangu.' 12 Licha ya kwamba
kweli ni dada yangu, binti wa baba yangu, ingawa si binti wa mama yangu; na ndiye
alifanyika kuwa mke wangu. 13 Wakati Mungu aliponiondoa katika nyumba ya baba
yangu na kusafiri kutoka mahali kwenda mahali pengine, nilimwambia mke wangu,
kwa kila sehemu tutakayo kwenda, unioneshe uaminifu wako kama mke wangu:
Kila mahali tutakapo kwenda, useme juu yangu kuwa, “Ni kaka yangu.”"' 14 Ndipo
Abimeleki akatwaa kondoo, maksai, watumwa wa kiume na wa kike akampatia
Abraham. Basi Abimeleki akamrudisha Sara, mke wa Abraham. 15 Abimeleki
akasema, Tazama, Nchi yangu i mbele yako. Kaa mahali utakapopendezewa.” 16 Na
kwa Sara akasema, Tazama, nimempatia kaka yako vipande elfu vya fedha. Navyo ni
kwa ajili ya kufunika kosa lolote dhidi yako machoni pa wote walio pamoja na wewe,
na mbele ya kila mtu ambaye umemfanya kuwa na haki.” 17 Kisha Abraham akaomba
kwa Mungu, Na Mungu akamponya Abimeleki, mkewe, na watumwa wake wa kike
kiasi kwamba wakaweza kupata watoto. 18 Kwa kuwa Yahwe alikuwa amewafanya
wanawake wote wa nyumaba ya Abimeleki kuwa tasa kabisa, kwa sababu ya Sara,
mke wa Abraham.

# 21

1 Yahwe akamsikiliza Sara kwa umakini kama alivyo kuwa amemwambia, Yahwe

akamfanyia Sara kama alivyo kuwa amemwahidi. [2] Sara akachukua mimba na
akamzalia Abraham mtoto wa kiume katika uzee wake, katika muda ule ule ambao
Mungu alikuwa amemwambia. [3] Abraham akamwita jina mwanawe, ambaye
alizaliwa kwake, na Sara, Isaka. [4] Abraham akamtahiri mwanawe Isaka alipofikisha
siku nane, kama vile Mungu alivyokuwa amemwagiza. [5] Abraham alikuwa na umri
wa miaka mia moja wakati mwanawe Isaka anazaliwa kwake. [6] Sara akasema,
“Mungu amenifanya nicheke; kila mtu atakaye sikia atacheka pamoja na nami.”
[7] Pia akasema, “Nani angesema kwa Abraham kwamba Sara atalea mtoto, na
sasa kweli nimemzalia mtoto wakiume katika uzee wake!” [8] Mtoto akakua na
akaachishwa kunyonya, na Abraham akafanya sherehe kubwa katika siku ambayo
Isaka aliachishwa. [9] Sara akamwona mwana wa Hajiri Mmisri, ambaye alikuwa
amezaliwa kwa Abraham, akidhihaki. [10] Kwa hiyo akamwambia Abraham, “Mfukuze
huyu mwanamke huyu mtumwa pamoja na mtoto wake: kwa kuwa mtoto huyu wa
mwanamke mtumwa hawezi kuwa mrithi pamoja na mwanangu Isaka.” [11] Jambo
hili likamuhuzunisha sana Abraham kwa sababu ya mwanawe. [12] Lakini Mungu
akamwambia Abraham, “Usihuzunike kwa sababu ya kijana huyu, na kwa sababu
ya mwanamke huyu mtumwa wako. Sikiliza maneno asemayo Sara juu ya jambo
hili, kwa sababu itakuwa kupitia Isaka kwamba uzao wako utaitwa. [13] Nitamfanya
pia mtoto wa mjakazi kuwa taifa, kwa sababu ni uzao wako.” [14] Abraham akaamka
asubuhi na mapema, akachukua mkate na kiriba cha maji, akampatia Hajiri, akiweka
juu ya bega lake. Akamtoa kijana akampatia Hajiri na akawaondoa. Hajiri
akaondoka akapotea katika jangwa la Beerisheba. [15] Maji yalipokwisha kwenye
kiriba akamtelekeza kijana katika moja ya vichaka. [16] Kisha akaondoka, na akakaa
umbali kidogo na yule kijana, umbali kama wa kutupa mshale, kwa vile alisema,
“Na nisitazame kifo cha mtoto.” Alipokuwa amekaa kumkabili, akapaza sauti yake
akalia. [17] Mungu akasikia kilio cha kijana, na malaika wa Mungu akamwita Hajiri
kutoka mbinguni, akamwambia, “Nini kinakusumbua? Usiogope, kwa kuwa Mungu
amesikia kilio cha kijana mahali alipo. [18] Inuka msimamishe mtoto, na umtie
moyo; kwa kuwa nitamfanya kuwa taifa kubwa.” [19] Kisha Mungu akayafunua
macho ya Hajiri, natazama akaona kisima cha maji. Akaenda akajaza kiriba maji,
na akampatia kijana akanywa. [20] Mungu akawa pamoja na kijana, na akakua.
Akaishi jangwani akawa mwindaji. [21] Akaishi katka jangwa la Parani, na mama
yake akampatia mke kutoka Misri. [22] Ikawa kwamba katika wakati ule Abimeleki
na Fikoli kamanda wa jeshi lake akamwambia Abraham, akisema, “Mungu yuko
pamoja na wewe katika yote uyatendayo. [23] Sasa niapie kwa Mungu kwamba
hutanifanyia baya, wala mwanangu, wala uzao wangu. Onesha kwangu na kwa
nchi ambayo umekuwa ukikaa agano lile lile la uaminifu ambalo nimekuonesha
wewe.” [24] Abraham akasema, “Nina apa.” [25] Abraham pia akamlalamikia Abimeleki
kuhusu kisima cha maji ambacho watumishi wa Abimeleki wamekinyang'anya.
[26] Abimeleki akasema, “Sijui ni nani amefanya jambo hili. Hukuniambia mapema; na
sijalisikia ila leo hii.” [27] Kwa hiyo Abraham akachukua kondoo na ng'ombe maksai
akampatia Abimeleki, na wawili hawa wakafanya agano. [28] Kisha Abraham akatenga
wanakondoo wa kike saba pekeyao. [29] Abimeleki akamwambia Abraham, “Nini
maana ya hawa wanakondoo wa kike saba ambao umewatenga pekeyao?” [30] Akajibu,
“Hawa wanakondoo wa kike saba utawapokea kutoka mkonono mwangu, ili kwamba
uwe ushahidi kwangu, kuwa nichimba kisima hiki.” [31] Kwa hiyo akaita mahali
pale Beerisheba, kwa sababu mahali pale wote wawili wali apa kiapo. [32] Walifanya
agano hapo Bersheba, kisha Abimeleki na Fikoli, amiri wa jeshi, wakarudi katika
nchi ya Wafilisti. [33] Abraham akapanda mti wa mkwaju katika Beerisheba. Na pale
akamwabudu Yahwe, Mungu wa milele. [34] Abraham akasalia kuwa mgeni katika nchi

ya Wafilisti kwa siku nyingi.

# 22

1 Ikawa kwamba baada ya mambo hayo Mungu akampima Abraham.
Akamwambia, “Abraham!” Abraham akasema, “Mimi hapa.” 2 Kisha Mungu
akasema, “Mchukue mwanao, mwanao wa pekee, umpendaye, Isaka, na uende katika
nchi ya Moria. Mtoe kama sadaka ya kuteketezwa mahali pale juu ya moja ya milima
hiyo, ambayo nitakwambia.” 3 Kwa hiyo Abraham akaamka asubuhi na mapema,
akatandika punda wake, akawachukuwa vijana wake wawili, pamoja na Isaka
mwanawe. Akakata kuni kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa, kisha akapanga safari
kwenda mahali ambapo Mungu alimwambia. 4 Siku ya tatu Abraham akatazama
juu na akaona mahali pakiwa mbali. 5 Abraham akawambia vijana wake, “kaeni
hapa pamoja na punda, mimi pamoja na Isaka tutakwenda pale. Tutaabudu na
kisha tutarudi hapa penu.” 6 Ndipo Abraham akachukua kuni kwa ajili ya sadaka ya
kuteketezwa akaziweka juu ya Isaka mwanawe. Mkononi mwake akachukua moto
na kisu; na wote wawili wakaondoka pamoja. 7 Isaka akazungumza na Abraham
baba yake akisema, “Baba yangu,” naye akasema, “ Ndiyo mwanangu.” Akasema,
“Tazama huu ni moto na kuni, lakini yuko wapi mwanakondoo kwa ajili ya sadaka ya
kuteketezwa?” 8 Abraham akasema, “Mungu mwenyewe atatupatia mwanakondoo
kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa, mwanangu.” Kwa hiyo wakaendelea, wote
wawili pamoja. 9 Walipofika mahali ambapo Mungu alikuwa amemwambia,
Abraham akajenga madhabahu pale na akaweka kuni juu yake. Kisha akamfunga
Isaka mwanawe, na akamlaza juu ya madhabahu, juu ya zile kuni. 10 Abraham
akanyoosha mkono wake akachukua kisu ili kumuua mwanawe. 11 Ndipo malaika
wa Yahwe akamwita kutoka mbinguni na kusema, “Abraham, Abraham!” naye
akasema, “Mimi hapa.” 12 Akasema, “usinyooshe mkono wako juu ya kijana, wala
usifanye jambo lolote kumdhuru, kwa kuwa sasa najua unamcha Mungu, kwa
kuona kuwa hukumzuilia mwanao, mwanao wa pekee, kwa ajili yangu.” 13 Abraham
akatazama juu na tazama, nyuma yake kulikuwa na kondoo mume amenaswa pembe
zake kichakani. Abraham akaenda akamchukua kondoo na akamtoa kama sadaka
ya kuteketezwa badala ya mwanawe. 14 Kwa hiyo Abraham akapaita mahali pale,
Yahwe atatoa,” na panaitwa hivyo hata leo. “Juu ya mlima wa Yahwe itatolewa.”
15 Malaika wa Yahwe akamwita Abraham kwa mara ya pili kutoka mbinguni 16 na
kusema - Hiki ni kiapo cha Yahwe, “Kwa ajili ya nafsi yangu nimeapa kwamba
kwa kuwa umefanya jambo hili, na hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee,
17 hakika nitakubariki na nitakuzidishia uzao wako kama nyota za angani, na kama
mchanga ulioko kwenye ufukwe wa bahari; na uzao wakowatamiliki lango la adui
zao. 18 Kupitia uzao wako mataifa yote ya dunia watabarikiwa, kwa sababu umetii
sauti yangu.” 19 Kwa hiyo Abraham akarejea kwa vijana wake, na wakaondoka
wakaenda pamoja Beerisheba, hivyo akakaa Beerisheba. 20 Ikawa kwamba baada
ya mambo haya ambayo Abraham aliambiwa, “Milka amemzalia pia watoto, ndugu
yako Nahori.” 21 Hawa walikuwa ni Usi mzaliwa wa kwanza, Busi ndugu yake,
Kemueli aliye mzaa Aramu, 22 Kesedi, Hazo, Pildashi, Yidlafu, na Bethueli. 23 Bethuel
akamzaa Rebeka. Hawa walikuwa ni wale watoto wanane ambao Milka alizaa kwa
Nahori, ndugu yake na Abraham. 24 Suria wake, ambaye aliitwa Reuma, pia akamzaa
Teba, Gahamu, Tahashi, na Maaka.

# 23

1 Sara akaishi mika mia moja na ishirini na saba. Hii ndiyo ilikuwa ni miaka
ya maisha ya Sara. 2 Sara akafa katika Kiriathi Arba, ambayo ni Hebroni, katika
nchi ya Kanaani. Abraham akaomboleza na kumlilia Sara. 3 Kisha Abraham

akainuka na kutoka kwa mkewe aliye kufa, akanena na watoto wa kiume wa
Hethi, akisema, 4 “Mimi ni mgeni kati yenu. Tafadhari nipatieni mahali pa kuzikia
miongoni mwenu, ili kwamba niweze kuzika wafu wangu.” 5 Wana wa Hethi
wakamjibu Abraham, wakasema, 6 “Tusikilize, bwana wangu. Wewe ni mwana wa
Mungu miongoni mwetu. Zika wafu wako katika makaburi yetu utakayochagua.
Hakuna miongoni mwetu atakaye kuzuilia kaburi lake, kwa ajili ya kuzikia wafu
wako.” 7 Abraham akainuka na kusujudu chini kwa watu wa nchi ile, kwa wana wa
Hethi. 8 Akawaambia, akisema, “ikiwa mmekubali mimi kuzika wafu wangu, ndipo
nisikilizeni, msihini Efroni mwana wa Sohari kwa ajili yangu. 9 Mwambieni aniuzie
pango la Makpela, ambalo analimiliki, ambalo liko mwishoni mwa shamba lake. Kwa
bei kamili aniuzie waziwazi mbele ya watu kama miliki ya kuzikia.” 10 Efroni alikuwa
ameketi miongoni mwa wana wa Hethi, hivyo Efroni Mhiti akamjibu Abraham
alipowasikia wana wa Hethi, wote ambao walikuwa wamekuja langoni mwa mji
wake, akasema, 11 “Hapana, bwana wangu, nisikilize. Ninakupatia shamba na pango
ambalo limo ndani yake. Ninakupatia mbele ya wana wa watu wangu. Ninakupatia
uzike wafu wako.” 12 Kisha Abraham akasujudu chini mbele ya watu wa nchi ile.
13 Akamwambia Efroni watu wa nchi ile wakisikiliza, akasema, ikiwa uko radhi,
tafadhari nisikilize. Nitalipia shamba. Chukua fedha kwangu, na nitazika wafu
wangu pale.” 14 Efroni akamjibu Abraham, akisema, 15 “Tafadhari bwana wangu,
nisikilize. Kipande cha ardhi kinathamani ya shekeli mia nne za fedha, na hiyo ni
kitu gani kati yangu mimi na wewe? wazike wafu wako.” 16 Abraham akamsikiliza
Efroni na akampimia Efroni kiwango cha fedha alizosema mbele ya wana wa Helthi
wakisikiliza, shekeli mia nne za fedha, kwa mujibu wa viwango vya vipimo vya
kibiashara. 17 Kwa hiyo shamba la Efroni, lililokuwa katika Makpela, mbele ya
Mamre, shamba pamoja na pango lililokuwamo ndani yake na miti yote iliyokuwamo
ndani ya shamba na iliyokuwa mpakani ikatolewa 18 kwa Abraham kwa njia ya
manunuzi mbele ya wana wa Hethi, na mbele ya wote waliokuja malangoni pa mji
wake. 19 Baada ya haya, Abraham akamzika Sara mkewe katika pango la shamba la
Makpela, lililo mbele ya Mamre, ambayo ni Hebroni, katika nchi ya Kanaani. 20 Kwa
hiyo shamba pamoja na pango likatolewa na wana wa Hethi kwa Abraham kama
milki na eneo la kuzikia.

# 24

1 Basi Abraham alikuwa mzee sana na Yahwe akawa amembariki katika mambo
yote. 2 Abraham akamwambia mtumwa wake, ambaye alikuwa mkubwa kuliko
wote wa nyumbani mwake na mkuu wa vyote alivyo kuwa navyo.”Weka mkono
wako chini ya paja langu 3 na nitakufanya uape kwa Yahwe, Mungu wa Mbingu
na nchi, kwamba hutampatia mwanangu mke kutoka kwa mabinti wa Wakanaani,
miongoni mwao wale nikaao kati yao. 4 Lakini utakwenda kwenye nchi yangu, na
kwa ndugu zangu, na kumtafutia mwanangu Isaka mke.” 5 Yule mtumwa wake
akamwambia, “Itakuwaje ikiwa mwanamke hatakuwa tayari kufuatana nami hadi
katika nchi hii? Je nitamrudisha mwanao katika nchi ambayo ulitoka?” 6 Abraham
akamwambia, “Hakikisha kwamba hutamrudisha mwanangu kule! 7 Yahwe, Mungu
wa mbingu, ambaye alinitoa mimi kutoka katika nyumba ya baba yangu na kutoka
katika nchi ya ndugu zangu, na ambaye aliniahidia kwa kiapo maalumu akisema,
'Nitawapa uzao wako nchi hii,' atatuma malaika wake mbele yako, na utapata mke
kwa ajili ya mwanangu kutoka huko. 8 Lakini ikiwa mwanamke hatakuwa tayari,
ndipo utakuwa huru katika hiki kiapo changu. Cha muhimu tu ni kwamba usije
ukamrudisha mwanangu huko.” 9 Kwa hiyo mtumwa akaweka mkono wake jini
ya paja la Abraham bwana wake, na akaapa kuhusiana na jambo hili. 10 Mtumwa

akachukua ngamia kumi wa bwana wake na akaondoka. Akachukua pia aina
zote za zawadi kutoka kwa bwana wake. Akaondoka na kwenda katika mkoa
wa Aramu Naharaimu, mji wa Nahori. 11 Akawapigisha magoti ngamia nje ya
mji karibu na kisima cha maji. Ilikuwa jioni wakati ambao wanawake huenda
kuchota maji. 12 Kisha akasema, “Yahwe, Mungu wa bwana wangu Abraham,
anijalie kufanikiwa leo na aoneshe agano la uaminifu kwa bwana wangu Abraham.
13 Tazama, nimesimama hapa karibu na chemchemi ya maji na binti za watu wa mji
wanakuja kuteka maji. 14 Na itokee hivi kwamba. Nikimwambia msichana, tafadhari
tua mtungi wako ili niweze kunywa maji,' na akiniambia, 'Kunywa, na kwamba
nitawanywesha ngamia wako pia,' huyo ndiye awe ambaye umemchagulia mtumwa
wako Isaka. Kwa njia hii nitajua kuwa umeonesha agano la uaminifu kwa bwana
wangu.” 15 Ikawa kwamba hata kabla hajamaliza kuzungumza, tazama, Rebeka akaja
akiwa na mtungi wake wa maji begani mwake. Rebeka alizaliwa na Bethueli mwana
wa Milka, mke wa Nahori, ndugu yake na Abraham. 16 Msichana huyu alikuwa
mzuri na alikuwa bikira. Hapana mwanaume aliye kuwa amekwisha lala naye.
Akashuka kisimani na kuujaza mtungi wake, na kupanda juu. 17 Kisha mtumwa
yule akakimbia kumlaki yule msichana, na kusema, “Tafadhari nipatie maji kidogo
ya kunywa kutoka katika mtungi wako.” 18 Akasema, “kunywa tafadhari bwana
wangu,” na kwa haraka akatua mtungi wake juu ya mkono wake, na akampatia maji
ya kunywa. 19 Alipokuwa amemaliza kumpatia maji, akasema, “Nitachota maji kwa
ajili ya ngamia wako pia, mpaka watakapomaliza kunywa.” 20 Hivyo akaharakisha
akamwaga maji yaliyokuwa mtungini kwenye chombo cha kunywshea mifugo, kisha
akakimbia tena kisimani kuchota maji, na kuwanywesha ngamia wake wote. 21 Yule
mtu akamtazama msichana akiwa kimya kuona kama Yahwe amefanikisha njia
yake au la. 22 Ngamia walipomaliza kunywa maji, yule mtu akaleta pete ya pua
ya dhahabu yenye uzito wa nusu shekeli, na bangili mbili za dhahabu kwa ajili
ya mikono yake zenye uzito wa shekeli kumi, 23 akamuuliza, “wewe ni binti wa
nani? Niambie tafadhali, Je kuna nafasi nyumbani mwa baba yako kwa ajili yetu
kupumzika usiku?” 24 Akamwambia, “Mimi ni binti wa Bethueli mwana wa Milka,
ambaye alimzaa kwa Nahori.” 25 Akasema pia, “Tunayo malisho tele na chakula,
na iko nafasi kwa ajili yako kulala usiku.” 26 Kisha yume mtu akainama chini
na kumwabudu Yahwe. 27 Akasema, “Abarikiwe Yahwe, Mungu wa bwana wangu
Abraham, ambaye hakuacha agano lake la uaminifu na kweli yake mbele ya bwana
wangu. Kwa vile Yahwe ameniongoza moja kwa moja kwenye nyumba ya ndugu
zake bwana wangu.” 28 Kisha yule msichana akakimbia na kwenda kuwaeleza watu
wa nyumba ya mama yake juu ya mambo yote haya. 29 Na sasa Rebeka alikuwa na
kaka yake, jina lake aliitwa Labani. Labani akakimbia kwa yule mtu aliye kuwa nje
barabarani karibu na kisima. 30 Akisha kuona hereni ya puani pamoja na zile bangili
kwenye mikono ya dada yake, na kusikia maneno ya Rebeka dada yake, “Hivi ndivyo
yule mtu alicho niambia,” alikwenda kwa yule mtu, na, Tazama, alikuwa amesimama
karibu na ngamia pale kisimani. 31 Labani akasema, “Njoo, wewe uliye barikiwa na
Yahwe. Kwa nini umesimama nje? nimekwisha andaa nyumba, pamoja na mahali
kwa ajili ya ngamia.” 32 Kwa hiyo yule mtu akaingia ndani ya nyumba na akashusha
mizigo kutoka kwa wale ngamia. Ngamia wakapatiwa malisho na chakula, na maji
yakatolewa kuosha miguu yake pamoja na miguu ya wale watu aliokuwa pamoja nao.
33 Wakaandaa chakula mbele yake ale, lakini akasema, “Sitakula mpaka niseme kile
ninacho paswa kusema.” Kwa hiyo Labani akmwambia, “Sema.” 34 Akasema, “Mimi
ni mtumwa wa Abraham. 35 Yahwe amembariki sana bwana wangu na amekuwa
mtu mkuu. Amempatia mifugo na makundi ya wanyama, fedha, dhahabu, watumwa
wa kiume na watumwa wa kike, pamoja na ngamia na punda. 36 Sara, mke wa bwana

wangu, alimzalia mwana bwana wangu alipokuwa mzee, na amempatia mwanawe
kila kitu anachomiliki. 37 Bwana wangu aliniapisha, akisema, “Usije ukampatia
mwanangu mke kutoka kwa mabinti wa Wakanaani, ambao kwao nimefanya makazi.
38 Badala yake, lazima uende kwa familia ya baba yangu, na kwa ndugu zangu,
na kupata mke kwa ajili ya mwanangu.' 39 Nikamwambia bwana wangu, pengine
mwanamke huyo asikubali kufuatana nami.' 40 Lakini akaniambia, Yahwe, ambaye
ninakwenda mbele yake, atatuma malaika wake pamoja nawe na atakufanikisha njia
yako, kwamba utapata mke kwa ajili ya mwangu kutoka miongoni mwa ndugu zangu
na kutoka katika ukoo wa baba yangu. 41 Lakini utakuwa huru katika kiapo changu
ikiwa utafika kwa ndugu zangu na wasikuruhusu kuja naye. Ndipo utakuwa huru
katika kiapo changu. 42 Hivyo nimefika leo kisimani, na nikasema, 'O Yahwe, Mungu
wa bwana wangu Abraham, tafadhari, ikiwa kweli umekusudia kuifanya safari yangu
kuwa yenye kufanikiwa - 43 tazama niko hapa nimesimama karibu na kisima cha
maji - na iwe kwamba binti ajaye kuchota maji, nitakaye mwambia, “Tafadhari
unipatie maji kidoka kutoka kwenye mtungi wako ninywe,” mwanamke atakaye
niabia, 44 “Kunywa, na nitakuchotea pia maji kwa ajili ya ngamia wako” - na awe
ndiye ambaye wewe Yahwe, umemchagulia mtoto wa bwana wangu.” 45 Ikawa hata
kabla sijamaliza kuzungumza moyoni mwangu, Tazama, Rebeka akaja na mtungi
wake juu ya bega lake akashuka chini kisimani akachota maji. Hivyo nikamwambia,
'Tafadhari nipatie maji ninywe.' 46 Ndipo kwa haraka alipoushusha mtungi wake
begani mwake na akasema, 'Kunywa, na pia nitawapatia maji ngamia wak.' Kwa
hiyo nikanywa, na akawanywesha ngamia pia. 47 Nikamuuliza na kusema, 'Wewe
ni binti wa nani?' Akasema, 'Binti wa Bethueli, Mwana wa Nahori, ambaye Milka
alizaa kwake.' Kisha nikamwekea pete puani mwake pamoja na bangili mikononi
mwake. 48 Kisha nikainama chini nikamwabudu Yahwe, na kumbariki Yahwe, Mungu
wa bwana wangu Abraham, ambaye ameniongoza katika njia sahihi kumpata binti
wa ndugu za bwana wangu kwa ajili ya mwanawe. 49 Kwa hiyo, ikiwa mko tayari
kumfanyia rehema na kweli, niambieni. Lakini kama sivyo, niambieni, ili kwamba
niweze kwenda upande wa kulia, au kushoto.” 50 Ndipo Labani na Bethueli wakajibu
na kusema, “Jambo hili limetoka kwa Yahwe; hatuwezi kusema kwako aidha neno
baya au zuri. 51 Tazama, Rebeka yu mbele yako. Mchukue na uende, ili awe mke wa
mtoto wa bwana wako, kama Yahwe alivyosema.” 52 Mtumwa wa Abraham aliposikia
maneno yao, akainama mwenyewe chini ardhini kwa Yahwe. 53 Mtumwa akaleta
vipande vya fedha na vipande vya dhahabu, na nguo, akampatia Rebeka. Akampatia
pia kaka yake na mama yake zawadi zenye thamani. 54 Kisha yeye na watu aliokuwa
nao wakala na kunywa. wakakaa pale mpaka usiku, na walipoamka asubuhi,
akasema, Niruhusuni niende kwa bwana wangu.” 55 Kaka yake na mama yake
wakasema, mwache binti abaki nasi kwa siku chache zingine, angalau siku kumi.
baada ya hapo anaweza kwenda.” 56 Lakini akawambia, msinizuie, kwa kuwa Yahwe
amefanikisha njia yangu. Niruhusuni niende kwa bwana wangu.” 57 Wakasema,
“Tutamwita binti na kumuuliza.” 58 Kwa hiyo wakamwita Rebeka na kumuuliza, “Je
utakwenda na mtu huyu?” Akajibu, “Nitakwenda.” 59 Kwa hiyo wakampeleka dada
yao Rebeka, pamoja na watumishi wake wa kike, kwenda njiani pamoja na mtumishi
wa Abraham na watu wake. 60 Wakambarikia Rebeka, na wakamwambia, “Ndugu
yetu, na uwe mama wa maelfu na wa makumi elfu, uzao wako upate kumiliki lango
la wale wanao wachukia.” 61 Kisha Rebeka akasimama, yeye na watumishi wake
kwa hesabu ya ngamia, na wakamfuata yule mtu. Hivyo watumishi wakamchukua
Rebeka, na wakaenda zao. 62 Nyakati hizo Isaka alikuwa anakaa katika Negebu, na
alikuwa tu amerejea kutoka Beerlahairoi. 63 Isaka akaenda kutafakari shambani
jioni. Alipotazama akaona, natazama, kulikuwa na ngamia wakija! 64 Rebeka

akatazama na alipomwona Isaka, akaruka kutoka kwenye ngamia. 65 Akamwambia
mtumwa, “mtu huyo ni nani anaye tembea shambani akija kutupokea?” Mtumwa
akasema, “Ni bwana wangu.” Hivyo Rebeka akachukua shela yake akajifunika.
66 Mtumwa akamwambia Isaka mambo yote ambayo amefanya. 67 Kisha Isaka
akamleta katika hema ya Sara mama yake na akamchukua Rebeka, na akawa mke
wake, na akampenda. Kwa hiyo Isaka akafarijika baada ya kifo cha mama yake.

# 25

1 Abraham akaoa mke mwingine; jina lake aliitwa Ketura. 2 Akamzalia Zimrani,
Jokshani, Medani, Midiani, Ishbaki, na Shua. 3 Jokshani akamzaa Sheba na Dedani.
Wana wa Dedani walikuwa ni Waashuru, Waletushi, na Waleumi. 4 Wana wa Midiani
walikuwa ni Efa, Eferi, Hanoki, Abida, na Eldaa. Hawa wote walikuwa ni wana wa
Ketura. 5 Abraham akampatia Isaka vitu vyote alivyokuwa navyo. 6 Ingawaje, wakati
alipokua angali akiishi, aliwapatia zawadi wana wa masuria wake na kuwapeleka
katika nchi ya mashariki, mbali na Isaka, mwanae. 7 Hizi ndizo zilikuwa siku za
miaka ya uhai wake Abraham alizoishi, miaka 175. 8 Abraham akapumua pumzi
ya mwisho na akafa katika uzee mwema, mzee aliye shiba siku, na akakusanywa
kwa watu wake. 9 Isaka na Ishmaili, wanae wakamzika katika pango la Makipela,
katika shamba la Efron mwana wa Soari Mhiti, pango lililokuwa karibu na Mamre.
10 Shamba hili Abraham alilinunua kwa watoto wa Hethi. Abraham akazikwa pale
pamoja na Sara mkewe. 11 Baada ya kifo cha Abraham, Mungu akambariki Isaka
mwanae, na Isaka akaishi karibu na Beerlalahairoi. 12 Na sasa hawa ndio walikuwa
wana wa Ishimaeli, mwana wa Abraham, ambaye Hajiri Mmisri mtumishi wake
Sara, alizaa kwa Abraham. 13 Haya ndiyo yalikuwa majina ya wana wa Ishimaeli,
kuanzia mzaliwa wa kwanza: Nebayothi - mzaliwa wa kwanza wa Ishimaeli, Kedari,
Adbeeli, Mibsamu, 14 Mishma, Duma, Masa, 15 Hadadi, Tema, Yeturi, Nafishi, na
Kedema. 16 Hawa ndio walikuwa wana wa Ishimaeli, na haya ndiyo majina yao,
kwa vijiji vyao, na katika vituo vyao; Maseyidi kumi na wawili kufuatana na kabila
zao. 17 Hii ndiyo ilikuwa miaka ya Ishimaeli, miaka 137: akapumua pumzi yake
ya mwisho na akafa, na akakusanywa pamoja na watu wake. 18 Walioshi toka
Havila mpaka Shuri, ambayo iko karibu na Misri, kuelekea Ashuru. Waliishi kwa
uadui kati yao. 19 Haya ndiyo yalikuwa matukio kumuhusu Isaka, mwana wa
Abraham: Abraham alimzaa Isaka. 20 Isaka alikuwa na umri wa miaka arobaini
alipomuoa Rebeka, binti wa ethueli Mshami wa Padani Aramu, ndugu wa Labani
Mshami. 21 Isaka akamwomba Yahwe kwa ajili ya mke wake kwa sababu alikuwa
tasa, na Yahwe akajibu maombi yake, Rebeka mkewe akabeba mimba. 22 Watoto
hawa walipokuwa tumboni mwake wakasumbuka, naye akasema, “Kwa nini jambo
hili linatokea kwangu mimi?” Akaenda kumuuliza Yahwe kuhusu jambo hili.
23 Yahwe akamwambia, “Mataifa mawili yako katika tumbo lako, na mataifa haya
mawili yatatengana ndani yako. Taifa moja litakuwa lenye nguvu kuliko lingine, na
yule mkubwa atamtumikia mdogo. 24 Ulipo wadia wakati wa kujifungua, tazama,
kulikuwa na mapacha ndani ya tumbo lake. 25 Wakwanza akatoka akiwa mwekundu
mwili wote kama vazi la nywele. Wakamwita jina lake Esau. 26 Baada ya hapo
ndugu yake akatoka. Mkono wake ukiwa umeshika kisigino cha Esau. Akaitwa
jina lake Yakobo. Isaka alikuwa na umri wa miaka sitini wakati mke wake alipo
wazaa hawa watoto. 27 Vijana hawa wakakua, Hesau akawa mwindaji hodari, mtu
wa nyikani; lakini Yakobo alikuwa mtu mkimya, aliye tumia muda wake akiwa katika
mahema. 28 Kisha Isaka akampenda Esau kwa sababu alikula wanyama ambao
alikuwa anawinda, lakini Rebeka akampenda Yakobo. 29 Yakobo akapika mchuzi.
Esau akaja kutoka nyikani, akiwa dhaifu kutokana na njaa. 30 Esau akamwambia

Yakobo, “Nilishe mchuzi mwekundu. Tafadhari, nimechoka!” Na hii ndiyo sababu
jina lake aliitwa Edomu. 31 Yakobo akasema, “Kwanza uniuzie haki yako ya mzaliwa
wa kwanza.” 32 Esau akasema, “Tazama, nakaribia kufa. Ni nini kwangu haki ya
mzaliwa wa kwanza?” 33 Yakobo akasema, “Kwanza uape kwangu mimi,” kwa hiyo
Esau akaapa kiapo na kwa njia hii akawa ameuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza
kwa Yakobo. 34 Yakobo akampatia Esau mkate pamoja na mchuzi wa dengu. Akala
na kunywa, kisha akainuka na akaenda zake. Kwa njia hii Esau akawa ameidharau
haki yake ya mzaliwa wa kwanza.

# 26

1 Basi njaa ikatokea katika nchi, mbali na njaa ya kwanza iliyotokea siku za
Ibrahimu. Isaka akaenda kwa Abimeleki, mfalme wa Wafilisiti huko Gerari.
2 Basi Yahwe akamtokea na kumwambia, “Usishuke kwenda Misri; kaa katika nchi
niliyokuambia. 3 Kaa katika nchi hii hii niliyokuambia, nami nitakuwa pamoja nawe
na kukubariki; kwani kwako wewe na uzao wako, nitawapa nchi hii yote, nami
nitatimiza kiapo nilichomwapia Ibrahimu baba yako. 4 Nitauzidisha uzao wako
kama nyota za mbinguni, nami nitawapa uzao wako nchi hizi zote. Kupitia uzao
wako mataifa yote ya dunia yatabarikiwa. 5 Nitalifanya hili kwa sababu Ibrahimu
aliitii sauti yangu na kutunza maelekezo yangu, amri zangu na sheria zangu.”
6 Hivyo Isaka akakaa Gerari. 7 Watu wa eneo hilo walipomwuliza juu ya mke wake,
alisema, “Yeye ni dada yangu.” Aliogopa kusema, “Yeye ni mke wangu,” kwa kuwa
alidhani, “Watu wa nchi hii wataniua ili wamchukue Rebeka, kwa kuwa ni mzuri
wa uso.” 8 Baada ya Isaka kuwa amekaa pale kwa muda mrefu, Ikatukia kwamba
Abimeleki mfalme wa Wafilisiti alichungulia katika dirisha. Tazama, akamwona
Isaka akimpapasa Rebeka, mke wake. 9 Abimeleki akamwita Isaka kwake na kusema,
“Tazama, kwa hakika yeye ni mke wako. Kwa nini ulisema, 'Yeye ni dada yangu?”
Isaka akamwambia, “Kwa sababu nilidhani mtu mmoja aweza kuniua ili amchukue.”
10 Abimeleki akamwambia, “Ni jambo gani hili ulilotufanyia? Mmojawapo wa watu
angeweza bila shaka kulala na mke wako, nawe ungeweza kuleta hatia juu yetu.”
11 Hivyo Abimeleki akawaonya watu wote na kusema, “Mtu yeyote atakayemgusa
mtu huyu au mke wake atauwawa.” 12 Isaka akapanda mazao katika nchi hiyo
na kuvuna mwaka huo vipimo mia, kwa kuwa Yahwe alimbariki. 13 Mtu huyo
akawa tajiri, naye akaongezeka zaidi hata akawa mkuu sana. 14 Alikuwa na kondoo
na ngombe na familia kubwa. Wafilisiti wakamwonea wivu. 15 Basi visima vyote
watumishi wa baba yake walikuwawamevichimba katika siku za Ibrahimu baba
yake, Wafilisiti wakavikatalia kwa kwa kuvijaza kifusi. 16 Abimeleki akamwambia
Isaka, “Ondoka kati yetu, kwa kuwa wewe una nguvu kuliko sisi.” 17 Hivyo Isaka
akaondoka pale na kukaa katika bonde la Gerari, na kuishi pale. 18 Kwa mara
nyingine tena Isaka akachimba visima vya maji, vilivyokuwa vimechimbwa siku za
Ibrahimu baba yake. Wafilisiti walikuwa wamevizuia baada ya kufa kwake Ibrahimu.
Isaka akaviita visima kwa majina aliyokuwa ameviita baba yake. 19 Watumishi
wa Isaka walipochimba katika bonde, wakaona kisima cha maji yaliyokuwakuwa
yakibubujika. 20 Wachungaji wa Gerari wakagombana na wachungaji wa Isaka,
na kusema, “Haya ni maji yetu.”Hivyo Isaka akakiita kisima hicho “Eseki,” kwa
sababu waligombana naye. 21 Wakachimba kisima kingine, wakakigombania hicho
nacho, hivyo akakiita “Sitina.” 22 Akatoka hapo na akachimba kisima kingine, lakini
hicho hawakukigombania. Hivyo akakiita Rehobothi, na akasema, “Sasa Yahwe
ametufanyia nafasi, na tutafanikiwa katika nchi.” 23 Kisha Isaka akaenda Beersheba.
24 Yahwe akamtokea usiku huohuo na akasema, “Mimi ni Mungu wa Ibrahimu
baba yako. Usiogope, kwa maana mimi nipo pamoja nawe na nitakubariki na

kuvidisha vizazi vyako, kwa ajili ya mtumishi wangu Ibrahimu.” 25 Isaka akajenga
madhabahu pale na akaliita jina la Yahwe. Akapiga hema yake pale, na watumishi
wake wakachimba kisima. 26 Kisha Abimeleki akamwendea kutoka Gerari, pamoja
na Ahuzathi, rafiki yake, na Fikoli, jemedari wa jeshi. 27 Isaka akawambia, “Kwa
nini mmekuja kwangu, kwani mlinichukia na kunifukuza kwenu. 28 Nao wakasema,
“Tumeona yakini kwamba Yahwe amekuwa nawe. Hivyo tukaamua kwamba kuwe
na kiapo kati yetu, ndiyo, kati yetu nawe. Hivyo na tufanye agano nawe, 29 kwamba
hautatudhuru, kama ambavyo sisi hatukukudhuru, na kama sisi tulivyokutendea
vema wewe na tumekuacha uondoke kwa amani. Kwa kweli, Yahwe amekubariki.”
30 Hivyo Isaka akawaandalia sherehe, na wakala na kunywa. 31 Wakaamuka
mapema asubuhi na wakaapiana kiapo. Kisha Isaka akawaruhusu kuondoka, nao
wakamwacha katika amani. 32 Siku hiyohiyo watumishi wake wakaja na kumwambia
juu ya kisima walichokuwa wamekichimba. Wakasema, “Tumeona maji.” 33 Akakiita
kile kisima Shiba, hivyo jina la mji ule ni Beersheba hata leo. 34 Esau alipokuwa na
umri wa miaka arobaini, akajitwalia mke, Yudithi binti Beeri Mhiti, na Basemathi
binti Eloni Mhiti. 35 Wakamhuzunisha Isaka na Rebeka.

# 27

1 Isaka alipozeeka na macho yake kuwa mazito kiasi cha kutokuona, alimwita Esau,
mwanawe mkubwa, na akamwambia, “Mwanangu. Yeye akasema, “Mimi hapa.”
2 Akamwambia, “Tazama, mimi nimezeeka. Sijui siku ya kufa kwangu. 3 Kwahiyo
chukua silaha zako, podo lako na upinde wako, na uende uwandani ukaniwindie
mnyama. 4 Uniandalie chakula kitamu, aina ile niipendayo, uniletee ili nikile na
kukubariki kabla sijafa. 5 Basi Rebeka akasikia Isaka alipoongea na Esau mwanawe.
Esau akaenda uwandani kuwinda mawindo na kuja nayo. 6 Rebeka akaongea na
Yakobo mwanawe na kumwambia, “Tazama, nimemsikia baba yako akiongea na
Esau ndugu yako. Akasema, 7 'Niletee mnyama na unitengenezee chakula kitamu,
ili nikile na kukubariki mbele za Yahwe kabla ya kufa kwangu.' 8 Kwa hiyo sasa,
mwanangu, usikilize sauti yangu kama ninavyokuagiza, 9 Nenda kundini, na uniletee
wanambuzi wawili; nami nitaandaa chakula kitamu kutokana nao kwa ajili ya baba
yako, kwa namna aipendayo. 10 Utakipeleka kwa baba yako, ili kwamba akile, na
kukubariki kabla hajafa.” 11 Yakobo akamwambia Rebeka mama yake, “Tazama,
Ndugu yangu Esau ni mtu mwenye manyoya, na mimi ni mtu laini. 12 Pengine baba
yangu atanigusa, nami nitaonekana kama mdanganyifu kwake. Nami nitajiletea
laana badala ya baraka.” 13 Mama yake akamwambia, “Mwanangu, acha laana
yoyote iwe juu yangu. Wewe sikiliza sauti yangu, nenda, uniletee.” 14 Hivyo Yakobo
alikwenda na kuchukua wanambuzi na kuwaleta kwa mama yake, na mama yake
akaandaa chakula kitamu, kama alichokipenda baba yake. 15 Rebeka akachukua
nguo nzuri za Esau, mwanawe mkubwa, alizokuwa nazo nyumbani mwake, na
akamvika Yakobo, mwanawe mdogo. 16 Akamvalisha ngozi ya mwanambuzi katika
mikono yake na katika sehemu laini za shingo yake. 17 Akaweka katika mikono ya
Yakobo kile chakula kitamu na mkate aliokuwa ameuandaa. 18 Yakobo akaenda kwa
baba yake na kumwambia, “Babangu.” Yeye akasema, “Mimi hapa; U nani wewe,
mwanangu?” 19 Yakobo akamwambia baba yake, “Mimi ni Esau mzaliwa wako wa
kwanza; nimefanya kama ulivyoniagiza. Basi kaa na ule sehemu ya mawindo yangu,
ili unibariki.” 20 Isaka akamwambia mwanawe, “Imekuwaje umepata kwa haraka
hivyo, mwanangu?” Akasema, “Ni kwa sababu Yahwe Mungu wako ameniletea.”
21 Isaka akamwambia Yakobo, “Njoo karibu nami, ili nikuguse, mwanangu, ili nijue
kama kweli wewe ni mwanangu Esau au hapana.” 22 Yakobo akamkaribia Isaka
baba yake; na Isaka akamgusa na kusema, “Sauti ni sauti ya Yakobo, lakini mikono

ni mkikono ya Esau.” [23] Isaka hakumtambua, kwa sababu mikono yake ilikuwa na
manyoya, kama mikono ya Esau ndugu yake, hivyo Isaka akambariki.” [24] Akasema,
“Wewe kweli ni mwanangu Esau?” Naye akasema, “Ni mimi.” [25] Isaka akasema,
“Kilete chakula kwangu, na nile mawindo yako, ili nikubariki.” Yakobo akakileta
chakula kwake. Isaka akala, na Yakobo akamletea mvinyo, akanywa. [26] Kisha Isaka
baba yake akamwambia, “Sogea karibu nami na unibusu, mwanangu.” [27] Yakobo
akasogea na kumbusu, naye akanusa harufu ya nguo zake na kumbariki. Akasema,
“Tazama, harufu ya mwanangu ni kama harufu ya shamba alilolibariki Yahwe.
[28] Mungu akupe sehemu ya umande wa mbinguni, sehemu ya unono wa nchi, na
wingi wa nafaka na mvinyo mpya. [29] Watu na wakutumikie na mataifa yainame
chini yako. Uwe bwana juu ya ndugu zako, na wana wa mama yako wainame
chini yako. Kila anayekulaani na alaaniwe; na kila anayekubariki abarikiwe.”
[30] Mara Isaka alipomaliza kumbariki Yakobo, na Yakobo ndo ametoka mbele ya
Isaka baba yake, Esau ndugu yake akaja kutoka kuwinda. [31] Yeye pia akaandaa
chakula kitamu na kukileta kwa baba yake. Akamwambia baba yake, “Baba, inuka
na ule baadhi ya mawindo ya mwanao, ili uweze kunibariki.” [32] Isaka baba yake
akamwambia, “U nani wewe? Akasema, “Mimi ni mwanao, Esau, mzaliwa wako wa
kwanza.” [33] Isaka akatetemeka sana na kusema, “Alikuwa nani aliyewinda mawindo
nakuniletea? Nilikula chote kabla haujaja, nami nimembariki. Atabarikiwa, kwa
kweli.” [34] Esau aliposikia maneno ya baba yake, akalia kwa kilio kikubwa na cha
uchungu sana, na akamwambia baba yake, “Unibariki nami, mimi pia, babangu.”
[35] Isaka akasema, “Ndugu yako alikuja hapa kwa hila na amechukua baraka yako.”
[36] Esau akasema, “Je hakuitwa Yakobo kwa haki? Kwa maana amenidanganya
mara mbili hizi. Alichukua haki ya uzaliwa wangu wa kwanza, na tazama, sasa
amechukua baraka yangu.” Na akasema, “Je haukuniachia baraka? [37] Isaka akajibu
na kumwambia Esau, “Tazama, nimemfanya kuwa bwana wako, na nimempa ndugu
zake kuwa watumishi wake. Na nimempa nafaka na divai. Je nikufanyie nini
mwanangu? [38] Esau akamwambia babaye, “Je hauna hata baraka moja kwa ajili
yangu, babangu? Nibariki nami, hata mimi pia, babangu.” Esau akalia kwa sauti.
[39] Isaka baba yake akajibu na kumwambia, “Tazama, mahali unapoishi patakuwa
mbali na utajiri wa nchi, mbali na umande juu angani. [40] Kwa upanga wako
utaishi, nawe utamtumikia ndugu yako. lakini utakapoasi, utaiondoa nira yake
shingoni mwako.” [41] Esau akamchukia Yakobo kwa sababu ya baraka ambayo baba
yake alimpa. Esau akajisemea moyoni, “Siku za maombolezo kwa ajili ya baba
yangu zinakaribia; baada ya hapo nitamwua Yakobo ndugu yangu.” [42] Rebeka
akaambiwa maneno ya Esau mwanawe mkubwa. Hivyo akatuma na kumwita Yakobo
mwanawe mdogo na kumwambia, “Tazama, Esau ndugu yako anajifariji juu yako
kwa kupanga kukuuwa. [43] Kwa hiyo sasa, mwanangu, unisikie na kukimbilia kwa
Labani, ndugu yangu, huko Harani. [44] Ukae naye kitambo, mpaka hasira ya ndugu
yako itakapopungua, [45] hata hasira ya ndugu yako itakapokuondokea, na kusahau
ulivyomtenda. Kisha nitatuma na kukurudisha kutoka pale. Kwa nini niwapoteze
ninyi nyote katika siku moja? [46] Rebeka akamwambia Isaka, “Nimechoka na maisha
kwa sababu ya hawa binti za Hethi. Ikiwa Yakobo atachukua mmojawapo wa binti wa
Hethi kuwa mkewe, kama wanawake hawa, baadhi ya binti za nchi, maisha yatakuwa
na maana gani kwangu?”

# 28

[1] Isaka akamwita Yakobo, akambariki, na kumwagiza, “Usichukuwe mwanamke
katika wanawake wa Kikanaani. [2] Inuka, nenda Padani Aramu, katika nyumba
ya Bethueli baba wa mama yako, na uchukue mwanamke pale, mmojawapo wa

binti za Labani, kaka wa mama yako. 3 Mungu Mwenyezi na akubariki, akupe
uzao na akuzidishe, hata uwe wingi wa watu. 4 Na akupe baraka ya Ibrahimu,
wewe, na uzao wako baada yako, kwamba uweze kumilki nchi ambapo umekuwa
ukiishi, ambayo Mungu alimpa Ibrahimu." 5 Hivyo Isaka akamwondoa Yakobo.
Yakobo akaenda Padani Aramu, kwa Labani mwana wa Bethueli Mwaramu, kaka wa
Rebeka, mama yao Yakobo na Esau. 6 Basi Esau alipoona kwamba Isaka amembariki
Yakobo na kumpeleka Padani Aramu, kuchukua mke kutoka pale. Lakini pia akaona
kwamba Isaka alikuwa amembariki na kumwagiza, akisema, "Usichukue mke katika
wanawake wa Kanaani." 7 Esau pia akaona kwamba Yakobo alikuwa amemtii baba
yake na mama yake, na alikuwa amekwenda Padani Aramu. 8 Esau akaona kwamba
wanawake wa Kanaani hawakumpendeza Isaka baba yake. 9 Hivyo akaenda kwa
Ishmaeli, na kuchukua, mbali na wake aliokuwa nao, Mahalathi binti Ishmaeli,
mwana wa Ibrahimu, dada wa Nebayothi, kuwa mke wake. 10 Yakobo akatoka
Beersheba na akaelekea Harani. 11 Akaja mahali fulani na akakaa pale usiku kucha,
kwa kuwa jua lilikuwa limekuchwa. Akachukua mojawapo ya mawe katika eneo hilo,
akaliweka chini ya kichwa chake, na akalala usingizi katika eneo hilo. 12 Akaota na
kuona ngazi imewekwa juu ya nchi. Ncha yake ilifika hata mbinguni na malaika wa
Mungu walikuwa wakishuka na kupanda juu yake. 13 Tazama, Yahwe amesimama
juu yake na kusema, "Mimi ni Yahwe, Mungu wa Ibrahimu baba yako, na Mungu wa
Isaka. Nchi uliyolala juu yake, nitakupa wewe na uzao wako. 14 Uzao wako utakuwa
kama mavumbi ya ardhi, na utaenea mbali kuelekea magharibi, mashariki, kaskazini,
na kusini. Kupitia kwako na kupitia uzao wako familia zote za dunia zitabarikiwa.
15 Tazama, mimi nipo nawe, na nitakulinda kila uendako, Nitakurudisha katika nchi
hii tena; kwani sitakuacha. Nitafanya kila nililokuahidi." 16 Yakobo akaamka katika
usingizi, na akasema, "Hakika Yahwe yupo mahali hapa, sikujua hili." 17 Akaogopa na
kusema, "Eneo hili linatisha kama nini! Hili sio kingine zaidi ya nyumba ya Mungu.
Hili ni lango la mbinguni." 18 Yakobo akaamka mapema asubuhi na akachukua jiwe
alilokuwa ameliweka chini ya kichwa chake. Akaliweka kama nguzo na kumimina
mafuta juu yake. 19 Akapaita pale Betheli, lakini jina la kawaida la mji lilikuwa
Luzu. 20 Yakobo akatoa nadhiri, kusema, "Ikiwa Mungu atakuwa nami na atanilinda
katika njia nipitayo, na atanipa mkate wa kula, na mavazi ya kuvaa, 21 hata nikarudi
salama katika nyumba ya baba yangu, ndipo Yahwe atakapokuwa Mungu wangu.
22 Kisha jiwe hili nililoliweka kama nguzo litakuwa jiwe takatifu. Kutoka katika kila
utakachonipa, kwa hakika nitakupa tena sehemu ya kumi."

# 29

1 Kisha Yakobo akaendelea na safari yake na akafika katika nchi ya watu wa
mashariki. 2 Hata alipotazama, akaona kisima kondeni, na, tazama, makundi
matatu ya kondoo yalikuwa yamelala kando yake. Kwani kutoka katika hicho
wangeyanywesha makundi, na jiwe juu ya mdomo wa kisima lilikuwa kubwa.
3 Wakati makundi yote yangekusanyika pale, wachungaji wangevingirisha jiwe
kutoka katika mdomo wa kisima na kuwanywesha kondoo, na kisha kurudisha jiwe
juu ya mdomo wa kisima, mahali pake. 4 Yakobo akawambia, "Ndugu zangu, ninyi
mnatokea wapi?" nao wakasema, "Tunatoka Harani." 5 Akawambia, "Mnamfahamu
Labani mwana wa Nahori?" Wakasema, "Tunamfahamu." 6 Akawambia, "Je
hajambo?" Wakasema, "Hajambo, na, tazama pale, Raheli binti yake anakuja na
kondoo." 7 Yakobo akasema, "Tazama, ni mchana. Siyo wakati wa kukusanya
kondoo pamoja. Mnapaswa kuwanywesha kondoo na kisha mkaenda na kuwaacha
wachunge." 8 Wakamwambia, "Hatuwezi kuwanywesha mpaka makundi yote
yakusanyike pamoja. Ndipo wanaume watakapovingirisha jiwe kutoka mlangoni

mwa kisima, na ndipo tutakapowanywesha kondoo." 9 Wakati bado Yakobo anaongea
nao, Raheli akaja pamoja na kondoo wa babaye, kwani alikuwa akiwachunga.
10 Yakobo alipomwona Raheli, binti wa Labani, kaka wa mamaye, na kondoo
wa Labani, kaka wa mama yake, Yakobo akaja juu, akalivingirisha jiwe kutoka
mlangoni mwa kisima, na akawanywesha kondoo wa Labani, kaka wa mama yake.
11 Yakobo akambusu Raheli na akalia kwa sauti. 12 Yakobo akamwambia Raheli
kwamba alikuwa ni ndugu wa baba yake, na kwamba alikuwa mwana wa Rebeka.
Kisha yeye akakimbia kumwambia baba yake. 13 Labani aliposikia habari kuhusu
Yakobo mwana wa dada yake, akaenda kukutana naye, akamkumbatia, akambusu,
na kumleta nyumbani kwake. Yakobo akamwambia Labani mambo haya yote.
14 Labani akamwambia, "Kwa hakika wewe ni mfupa wangu na nyama yangu."
Kisha Yakobo akakaa naye kama mwezi mmoja. 15 Kisha Labani akamwambia
Yakobo, "Je unitumikie bure kwa kuwa wewe ni ndugu yangu? Niambie, ujira wako
utakuwaje? 16 Basi Labani alikuwa na binti wawili. Jina la mkubwa lilikuwa ni
Lea, na jina la mdogo lilikuwa Raheli. 17 Macho ya Lea yalikuwa dhaifu, lakini Raheli
alikuwa mzuri wa umbo na mwonekano. 18 Yakobo alimpenda Raheli, hivyo akasema,
"Nitakutumikia miaka saba kwa ajili ya Raheli, binti yako mdogo." 19 Labani
akasema, Itakuwa vema kukupa wewe, kuliko kumpa mtu mwingine. Kaa nami."
20 Hivyo Yakobo akamtumikia kwa miaka saba kwa ajili ya Raheli; nayo ilionekana
kwake kama siku chache tu, kwa ajili ya upendo aliokuwa nao kwake. 21 Kisha
Yakobo akamwambia Labani, "Nipe mke wangu, kwani siku zangu zimetimia - ili
kwamba nimwoe! 22 Hivyo Labani akawaalika watu wa mahali hapo na kuandaa
sherehe. 23 Wakati wa jioni, Labani akamchukua Lea binti yake mkubwa na kumleta
kwa Yakobo, aliyelala naye. 24 Labani akampa mtumishi wake wakike Zilpa kuwa
mjakazi wa Lea. 25 Ilipofika asubuhi, tazama, kumbe ni Lea! Yakobo akamwambia
Labani, "Ni nini hiki ulichonifanyia? Je sikukutumikia kwa ajili ya Raheli? Kwa
nini basi umenihadaa? 26 Labani akamwambia, "Siyo utamaduni wetu kumtoa bindi
mdogo kabla ya mzaliwa wa kwanza. 27 Timiza juma la bibi arusi, na tutakupa
yule mwingine pia kwa mbadala wa kunitumikia miaka mingine saba." 28 Yakobo
akafanya hivyo, na akatimiza juma la Lea. Kisha Labani akampa Raheli binti yake
kuwa mke wake. 29 Lakini pia Labani akampa Raheli binti yake Bilha, kuwa mjakazi
wake. 30 Hivyo Yakobo akalala na Raheli, pia, lakini akampenda Raheli zaidi ya
Lea. Hivyo Yakobo akamtumikia Labani kwa miaka saba mingine. 31 Yahwe akaona
kwamba Lea hakupendwa, hivyo akalifungua tumbo lake, lakini Raheli hakuwa na
mtoto. 32 Lea akashika mimba na kuzaa mwana, naye akamwita Rubeni. Kwani
alisema, "Kwa sababu Yahwe ameliangalia teso langu; bila shaka mme wangu sasa
atanipenda." 33 Kisha akashika mimba tena na kuzaa mwana. Akasema, "Kwa
sababu Yahwe amesikia kwamba sipendwi, kwa hiyo amenipa mwana mwingine," na
akamwita Simoni. 34 Kisha akashika mimba tena na kuzaa mwana. Akasema, "Wakati
huu mme wangu ataungana nami, kwa kuwa nimemzalia wana watatu." Kwa hiyo
akaitwa Lawi. 35 Akashika mimba tena na kuzaa mwana. Akasema, "Wakati huu
nitamsifu Yahwe." Kwa hiyo akamwita jina lake Yuda; kisha akaacha kuzaa watoto.

# 30

1 Raheli alipoona kwamba hamzalii Yakobo watoto, Raheli akamwonea wivu dada
yake. Akamwambia Yakobo, "Nipe watoto, sivyo nitakufa." 2 Hasira ya Yakobo
ikawaka juu ya Raheli. Akasema, "Mimi ni badala ya Mungu, aliyekuzuilia usipate
watoto? 3 Akasema, "Tazama, kuna mjakazi wangu Bilha. Lala naye, hivyo aweze
kuzaa watoto magotini pangu, nami nitapata watoto kwake. 4 Hivyo akampa Bilha
mjakazi kama mke wake, na Yakobo akalala naye. 5 Bilha akashika mimba na

kumzalia Yakobo mwana. 6 Kisha Raheli akasema, “Mungu ameamua kwa faida
yangu. Ameyasikiliza maombi yangu na kunipa mwana.” Kwa sababu hiyo akamwita
jina lake Dani 7 Bilha, mjakazi wa Raheli, akashika mimba tena na kumzalia Yakobo
mwana wa pili. 8 Raheli akasema, “Kwa mashindano yenye nguvu nimeshindana
na dada yangu na kushinda.” Akamwita jina lake Naftali. 9 Lea alipoona kwamba
ameacha kuzaa, akamchukua Zilpa, mjakazi wake, na kumpa Yakobo kama mke
wake. 10 Zilpa, mjakazi wa Lea, akamzalia Yakobo mwana. 11 Lea akasema, “Hii
ni bahati njema!” Hivyo akamwita jina lake Gadi. 12 Kisha Zilpa, mjakazi wa Lea,
akamzalia Yakobo mwana wa pili. 13 Lea akasema, “Nina furaha! Kwa maana mabinti
wataniita furaha.” Hivyo akamwita jina lake Asheri. 14 Siku za mavuno ya ngano
Rubeni akaenda shambani na kuona tunguja. Akazileta kwa mama yake. Kisha
Raheli akamwambia Lea, “Nipe baadhi ya tunguja za mwanao.” 15 Lea akamwambia,
“Je ni jambo dogo kwako, kumchukua mme wangu? Je na sasa unataka kuchukua
tunguja za mwanangu pia? Raheli akasema, “Kisha atalala nawe leo usiku, kwa
kubadilishana na tunguja za mwanao. 16 Jioni Yakobo akaja kutoka uwandani.
Lea akaenda kumlaki na kusema, “Leo usiku utalala nami, kwani nimekuajiri kwa
tunguja za mwanangu.” Hivyo Yakobo akalala na Lea usiku huo. 17 Mungu akamsikia
Lea, na akashika mimba na kumzalia Yakobo mwana wa tano. 18 Lea akasema,
“Mungu amenipa ujira wangu, kwa sababu nilimpa mme wangu mjakazi wangu.”
Akamwita jina lake Isakari. 19 Lea akashika mimba tena na kuzaa mwana wa tano
kwa Yakobo. 20 Lea akasema, “Mungu amenipa zawadi njema. Sasa mme wangu
ataniheshimu, kwa sababu nimemzalia wana sita.” Akamwita jina lake Zabuloni.
21 Baadaye akazaa binti na kumwita jina lake Dina. 22 Mungu akamkumbuka Raheli
na kumsikiliza. Akampa kushika mimba. 23 Akashika mimba na kuzaa mwana.
Akasema, “Mungu ameiondoa aibu yangu.” 24 Akamwita jina lake Yusufu, akisema,
Yahwe ameniongeza mwana mwingine.” 25 Baada ya Raheli kumzaa Yusufu, Yakobo
akamwambia Labani, “Niache niande, ili kwamba niende nyumbani kwetu na katika
nchi yangu. 26 Nipe wake zangu na watoto wangu niliokutumikia kwa ajili yao,
na uniache niondoke, kwani unafahamu nilivyokutumikia. 27 Labani akamwambia,
“Ikiwa nimepata kibali machoni pako, subiri, kwa sababu nimejifunza kwa kutumia
uaguzi kwamba Yahwe amenibariki kwa ajili yako.” 28 Kisha akasema, “Taja ujira
wako, nami nitalipa.” 29 Yakobo akamwambia, “Unajua nilivyokutumikia, na jinsi
ambavyo mifugo wako wamekuwa nami. 30 Kwani walikuwa wachache kabla sijaja,
na wameongezeka kwa wingi. Popote nilipokutumikia Mungu amekubariki. Je ni
lini mimi nitaandaa kwa ajili ya nyumba yangu pia?” 31 Hivyo Labani akasema,
“Je nikulipe nini? Yakobo akasema, 'Usinipe chochote. Ikiwa utafanya jambo hili
kwa ajili yangu, nitawalisha tena kondoo wako na kuwatunza. 32 Niache nipite
kati ya kundi lako lote leo, kwa kuondoa kila kondoo mwenye milia na mabaka,
na kila kondoo mweusi kati yao, na kati ya wenye mabaka na milia katika mbuzi.
Hawa watakuwa ujira wangu. 33 Uadilifu wangu utashuhudia kwa ajili yangu hapo
baadaye, utakapokuja kuangalia ujira wangu. Kila ambaye hana milia na hana madoa
miongoni mwa mbuzi, na mweusi kati ya kondoo, ikiwa wataonekana kwangu,
watahesabiwa kuwa wameibwa.” 34 Labani akasema, “Nakubali. Na iwe kama
yalivyo maneno yako.” 35 Siku hiyo Labani akaondoa mabeberu yaliyokuwa na
milia na madoa, na majike ya mbuzi yaliyokuwa na milia na madoa, kila aliyekuwa
mweupe, na weusi wote katika mbuzi, akawakabidhi katika mikono ya wanaye. 36 Pia
Labani akaweka safari ya siku tatu kati yake na Yakobo. Hivyo Yakobo akabaki
kuchunga wale kondoo wa Labani waliosalia. 37 Yakobo akachukua matawi mabichi
yaliyokatwa ya mipopla, mlozi na mwaramoni mbichi akatoa maganda ili michilizi
myeupe ionekane, na akaifanya sehemu nyeupe ya ndani ya mti iliyokuwa ndani ya

fito ionekane. 38 Kisha akaziweka fito alizokuwa amezibambua mbele ya makundi
ya kondoo, mbele ya mabirika yakunyweshea walipokuja kunywa maji. Wakashika
mimba walipokuja kunywa maji. 39 Wanyama wakapandana mbele ya fito; nao
wakazaa watoto wenye milia, mabaka na wenye madoa. 40 Yakobo akawatenga
hawa wanakondoo, lakini akawafanya waliosalia kuelekea wanyama wenye milia
na kondoo weusi wote katika kundi la Labani. Kisha akayatenga makundi yake
mwenyewe pekee na hakuwaweka pamoja na wale wa Labani. 41 Pindi kondoo
wenye nguvu katika kundi walipopandana, Yakobo alilaza fito katika mabirika ya
maji mbele ya macho ya kundi, ili kwamba washike mimba kati ya fito. 42 Lakini
wakati waliodhaifu walipokuja, hakuweka fito mbele yao. Hivyo wanyama dhaifu
wakawa wa Labani, na wenye nguvu wakawa wa Yakobo. 43 Mtu huyo akastawi
sana. Akawa na kundi kubwa la kondoo, wajakazi na wajoli, ngamia na punda.

# 31

1 Basi Yakobo akasikia maneno ya wana wa Labani, wakisema, “Yakobo
amechukuwa yote yaliyokuwa ya baba yetu, na ni kutoka katika mali ya baba yetu
amepata utajiri wake.” 2 Yakobo akaona mwonekano katika uso wa Labani. Akaona
kwamba nia yake imebadilika. 3 Kisha Yahwe akamwambia Yakobo, “Rudi katika nchi
ya baba zako na ya ndugu zako, nami nitakuwa nawe.” 4 Yakobo akatuma kuwaita
Raheli na Lea uwandani katika kundi lake la kondoo 5 naye akawambia, “Naona
nia ya baba yenu kwangu imebadilika, lakini Mungu wa baba yangu amekuwa
nami. 6 Nanyi mnajua kwamba ni kwa nguvu zangu zote nimemtumikia baba yenu.
7 Baba yenu amenidanganya na amebadilisha ujira wangu mara kumi, lakini Mungu
hakumruhusu kunidhuru. 8 Ikiwa alisema, 'Wanyama wenye mabaka watakuwa ujira
wako,' ndipo kondoo wote walipozaa watoto wenye mabaka. Na aliposema, wenye
milia watakuwa ujira wako,' ndipo kundi lote lilipozaa watoto wenye milia. 9 Kwa
njia hii Mungu amemnyang'anya mifugo baba yenu na kunipa mimi. 10 Wakati fulani
wa majira ya kupandana, niliona katika ndoto mabeberu yaliyowapanda kundi.
Mabeberu yalikuwa ya milia, mabaka na madoa. 11 Malaika wa Mungu akaniambia
katika ndoto, 'Yakobo.' Nikasema, 'Mimi hapa.' 12 Akasema, 'Inua macho yako uone
mabeberu wanaolipanda kundi. Wana milia, madoa na na mabaka, kwani nimeona
kila jambo Labani analokutendea. 13 Mimi ni Mungu wa Betheli, mahali ulipoitia
nguzo mafuta, mahali uliponitolea nadhiri. Basi sasa inuka na uondoke katika nchi
hii na kurudi katika nchi uliyozaliwa. 14 Raheli na Lea wakajibu na kumwambia, “Je
kuna sehemu yoyote au urithi wetu katika nyumba ya baba yetu? 15 Je hatutendei
kama wageni? Kwa maana ametuuza na kwa ujumla ametapanya pesa zetu. 16 Mali
zote ambazo sasa Mungu amemnyang'anya baba yetu ni zetu na watoto wetu. Sasa
basi, lolote Mungu alilokuambia, fanya. 17 Kisha Yakobo akainuka na kuwapandisha
wanawe na wakeze kwenye ngamia. 18 Akawaongoza mifugo wake wote mbele yake,
pamoja na mali zake zote, wakiwemo wanyama aliowapata huko Padani Aramu.
Kisha akaenda kuelekea kwa Isaka baba yake katika nchi ya Kanaani. 19 Labani
alipokuwa amekwenda kuwakata manyoya kondoo wake, Raheli akaiba miungu
ya nyumba ya baba yake. 20 Yakobo pia akamdanganya Labani Mwarami, kwa
kutomtaarifu kwamba anaondoka. 21 Hivyo akaondoka na vyote alivyokuwa navyo
na kwa haraka akavuka mto, na akaenda kuelekea nchi ya vilima ya Gileadi. 22 Siku
ya tatu Labani akaambiwa kwamba Yakobo amekimbia. 23 Hivyo akawachukua
ndugu zake pamoja naye na kumfuatia kwa safari ya siku saba. Akampata katika nchi
ya vilima ya Gileadi. 24 Basi Mungu akaja kwa Labani Mwarami katika ndoto usiku
na kumwambia, “Ujiadhari kumwambia Yakobo jambo lolote liwe jema au baya.”
25 Labani akampata Yakobo. Basi Yakobo alikuwa amepiga hema yake katika nchi

ya vilima. Labani pia akapiga kambi pamoja na ndugu zake katika nchi ya kilima
ya Gileadi. 26 Labani akamwambia Yakobo, “Umefanya nini, kwamba umewachukua
binti zangu kama mateka wa vita? 27 Kwa nini umekimbia kwa siri na kunihadaa
kwa kutokuniambia? Ningekuruhusu uondoke kwa sherehe na kwa nyimbo, kwa
matari na vinubi. 28 Haukuniacha niwabusu wajukuu wangu na binti zangu kwa
kuwaaga. Basi umefanya upumbavu. 29 Iko katika uwezo wangu kukudhuru,
lakini Mungu wa baba yako alisema nami usiku wa leo na kuniambia, 'Jiadhari
usimwambie Yakobo neno la heri wala shari.' 30 Na sasa, umeondoka kwa sababu
umeitamani sana nyumba ya baba yako. Lakini kwa nini umeiba miungu yangu?
31 Yakobo akajibu na kumwambia Labani, “Ni kwa sababu niliogopa na kudhani kuwa
ungeninyang'anya binti zako kwa nguvu ndiyo maana nikaondoka kwa siri. 32 Yeyote
aliyeiiba miungu yako hataendelea kuishi. Mbele ya ndugu zetu, onesha chochote
kilichochako nilichonacho na uchukue.” Kwa maana Yakobo hakujua kwamba Raheli
alikuwa ameviiba. 33 Labani akaingia katika hema ya Yakobo, katika hema ya Lea,
na katika hema za wale wajakazi wawili, lakini hakuviona. Akatoka katika hema ya
Lea na kuingia katika hema ya Raheli. 34 Basi Raheli alikuwa ameichukua miungu ya
nyumbani, na kuiweka katika ngozi ya ngamia, na kukaa juu yake. Labani akatafuta
katika hema yote, lakini hakuiona. 35 Akamwambia baba yake, “Usikasirike, bwana
wangu, kwamba siwezi kusimama mbele yako, kwani nipo katika kipindi changu.”
Hivyo akatafuta lakini hakuiona miungu ya nyumbani mwake. 36 Yakobo akakasirika
na kuojiana na Labani. Akamwambia, “Kosa langu ni nini? Dhambi yangu ni ipi, hata
ukanifuatia kwa ukali? 37 Kwa maana umechunguza mali zangu zote. Umeona nini
kati ya kitu chochote cha nyumbani mwako? Viweke hapa mbele ya ndugu zetu, ili
waamue kati yetu wawili. 38 Kwa miaka ishirini nimekuwa nawe. Kondoo wako na
mbuzi wako hawakutoa mimba, wala sikula dume lolote la kondoo katika wanyama
wako. 39 Kilichoraruliwa na hayawani sikukuletea. Badala yake, nilichukua upotevu
huo, kwamba wameibwa mchana au usiku. 40 Nilikuwepo wakati wote; mchana
joto lilinipata, na baridi wakati wa usiku; na sikupata usingizi. 41 Miaka hii ishirini
nimekuwa katika nyumba yako. Nilikufanyia kazi miaka kumi na nne kwa ajili
ya binti zako wawili, na miaka sita kwa ajili ya wanyama wako. Umebadili ujira
wangu mara kumi. 42 Isipokuwa Mungu wa baba yangu, Mungu wa Ibrahimu, yule
Isaka anayemwofu, amekuwa nami, bila shaka sasa ungenipeleka mikono mitupu.
Mungu ameliona teso langu na jinsi nilivyofanya kazi kwa bidii, na hivyo akakukemea
usiku wa leo. 43 Labani akajibu na kumwambia Yakobo, “Mabinti hawa ni mabinti
zangu, wajukuu ni wajukuu wangu, na wanyama ni wanyama wangu. Yote uyaonayo
ni yangu. Lakini nitafanya nini leo kwa hawa binti zangu, au kwa watoto wao
waliowazaa? 44 Hivyo sasa, na tufanye agano, wewe nami, na liwe shahidi kati
yangu nawe.” 45 Hivyo Yakobo akachukua jiwe na kuliweka kama nguzo. 46 Yakobo
akawambia ndugu zake, “Kusanyeni mawe.” Hivyo wakachukua mawe na kufanya
rundo. Kisha wakala pale kati ya lile rundo. 47 Labani aliliita Yega Saha Dutha,
lakini Yakobo akaiita Galeedi 48 Labani akasema, “Rundo hili ni shahidi kati yangu
nawe leo.” Kwa hiyo jina lake likaitwa Galedi. 49 Inaitwa pia Mispa, kwa sababu
Labani alisema, “Yahwe na atuangalie mimi nawe, tunapokuwa hatuonani. 50 Ikiwa
utawatesa binti zangu, au ikiwa utachukua wanawake wengine mbali na binti zangu,
japokuwa hakuna mwingine yupo nasi, tazama, Mungu ni shahidi kati yangu nawe.”
51 Labani akamwambia Yakobo, Tazama rundo hili, na tazama nguzo, nililoliweka
kati yako nami. 52 Rundo hili ni shahidi, na nguzo ni shahidi, kwamba sitapita rundo
hili kuja kwako, na kwamba wewe hautapita rundo hili kuja kwangu, kwa madhara.
53 Mungu wa Ibrahimu, na mungu wa Nahori, miungu ya baba zao, waamue kati
yetu.”Yakobo akaapa kwa Hofu ya Isaka baba yake. 54 Yakobo akatoa sadaka juu ya

mlima na akawaita ndugu zake kula chakula. Walikula na kukaa usiku kucha juu
ya mlima. 55 Labani akaamka asubuhi na mapema, akawabusu wajuu zake na binti
zake na kuwabariki. Kisha Labani akaondoka na kurudi kwake.

# 32

1 Yakobo pia akaendelea na safari yake, na malaika wa Mungu wakakutana
naye. 2 Yakobo alipowaona, akasema, “Hii ni kambi ya Mungu,” hivyo akapaita
mahali pale Mahanaimu. 3 Yakobo akatuma wajumbe mbele yake waende kwa
Esau ndugu yake katika nchi ya Seiri, katika eneo la Edomu. 4 Aliwaagiza, kusema,
“Hivi ndivyo mtakavyosema kwa bwana wangu Esau: Hivi ndivyo mtumishi wako
Yakobo asemavyo: 'Nimekuwa nikikaa na Labani, naye amekawilisha kurudi kwangu
hata sasa. 5 Nina ng'ombe, punda, na kondoo, wajori na wajakazi. Nimetuma
ujumbe huu kwa bwana wangu, ili kwamba nipate kibali mbele zako.” 6 Wajumbe
wakarudi kwa Yakobo na kusema, “Tulikwenda kwa Esau ndugu yako. Anakuja
kukulaki, na watu mia nne pamoja naye.” 7 Ndipo Yakobo alipoogopa sana na
kutaabika. Hivyo akagawanya watu aliokuwa nao katika kambi mbili, na kondoo pia,
mbuzi na ngamia. 8 Akasema, “Ikiwa Esau ataishambulia kambi moja, ndipo kambi
nyingine itakaposalimika.” 9 Yakobo akasema, “Mungu wa baba yangu Ibrahimu,
na Mungu wa baba yangu Isaka, Yahwe, uliyeniambia, 'Rudi katika nchi yako na
kwa jamaa yako, nami nitakustawisha,' 10 Mimi sistahili matendo yako yote ya agano
la uaminifu na ustahilifu wote uliomfanyia mtumishi wako. Kwa maana nilikuwa
na fimbo tu nilipovuka mto huu wa Yordani, na sasa nimekuwa matuo mawili.
11 Tafadhari niokoe kutoka katika mikono ya ndugu yangu, mikono ya Esau, kwa
maana namwogopa, kwamba atakuja na kunishambulia mimi na wamama na watoto.
12 Lakini ulisema, 'hakika nitakufanya ufanikiwe. Nitaufanya uzao wako kuwa kama
mchanga wa bahari, ambao hauwezi kuhesabika kwa hesabu yake.” 13 Yakobo
akakaa pale usiku huo. Akachukua baadhi ya alivyokuwa navyo kama zawadi
kwa Esau, ndugu yake: 14 mbuzi majike mia mbili na mabeberu ishirini, kondoo
majike mia mbili na madume ya kondoo ishirini, 15 ngamia wakamwao thelathini
na wana wao, ng'ombe madume arobaini na madume kumi ya ng'ombe, punda wa
kike ishirini na madume yake ishirini. 16 Akawaweka katika mikono ya watumishi
wake, kila kundi peke yake. Akawambia watumishi, “Tangulieni mbele yangu na
mwache nafasi kati ya makundi ya wanyama.” 17 Akamwagiza mtumishi wa kwanza,
akisema, “Ndugu yangu Esau atakapokutana nawe na kukuuliza, akasema, 'Ninyi ni
wa nani? Mnakwenda wapi? Na wanyama hawa mbele yenu ni wa nani? 18 Ndipo
umwambie, 'Ni wa mtumishi wako Yakobo. Ni zawadi wanaopelekwa kwa bwana
wangu Esau. Na tazama, yeye pia anakuja nyuma yetu.” 19 Yakobo akatoa maelekezo
kwa kundi la pili pia, la tatu, na watu wote walioyafuata makundi ya wanyama.
Akasema, mseme vilevile kwa Esau mtakapokutana naye. 20 Mnapaswa pia kusema,
'mtumwa wako Yakobo pia anakuja nyuma yetu.” Kwani alifikiri, “nitamtuliza
Esau kwa zawadi nilizozituma mbele yangu. Kisha baadaye, nitakapomwona, bila
shaka atanipokea.” 21 Hivyo zawadi zikatangulia mbele yake. Yeye mwenyewe
akakaa kambini usiku huo 22 Yakobo akaamka wakati wa usiku, na akawachukua
wakeze, wajakazi wake na wanaye kumi na wawili. Akawawavusha kijito cha
Yaboki. 23 Kwa njia hii akawapeleka kupitia chemichemi pamoja na mali yake yote.
24 Yakobo akaachwa peke yake, na mtu akashindana naya mpaka alfajiri. 25 Mtu
yule alipoona kwamba hawezi kumshinda, akalipiga paja lake. Paja la Yakobo
likatenguka alipokuwa akishindana naye. 26 Yule mtu akasema, “Niache niende,
kwani kunakucha.” Yakobo akasema, sitakuacha uende mpaka uwe umenibariki.”
27 Yule mtu akamwuliza, “Jina lako ni nani?” Yakobo akasema, “Yakobo.” Yule mtu

akasema, [28] "Jina lako halitakuwa Yakobo tena, ila Israeli. Kwa kuwa umeshindana na
Mungu na wanadamu na umeshinda." [29] Yakobo akamwambia, "Tafadhari niambie
jina lako." Akasema, "Kwa nini kuniuliza jina langu?" Kisha akambariki pale.
[30] Yakobo akapaita mahali pale Penieli kwani alisema, "Nimemwona Mungu uso kwa
uso, na maisha yangu yamesalimika." [31] Jua likatoka wakati Yakobo anaipita Penieli.
Alikuwa akichechemea kwa sababu ya paja lake. [32] Ndiyo maana wana wa Israeli
hawali kano ya paja iliyopo katika nyonga ya paja, kwa sababu yule mtu aliziumiza
hizo kano alipotegua paja la Yakobo.

# 33

[1] Yakobo akainua macho yake na, tazama, Esau alikuwa anakuja, na alikuwa na
watu mia nne pamoja naye. Yakobo akawagawanya watoto kati ya Lea, Raheli, na
wale wajakazi wawili. [2] Kisha akawaweka wajakazi na wanao mbele, wakifuatiwa
na Lea na watoto wake, Raheli na Yusufu wakafuata mwisho wa wote. [3] Yeye
mwenyewe akatangulia mbele yao. Akasujudu mara saba kuelekea ardhi, hata
alipomkaribia ndugu yake. [4] Esau akakimbia kumlaki, akamkumbatia, akakumbatia
shingo yake na kumbusu. Kisha wakalia. [5] Esau alipoinua macho, aliona wanawake
na watoto. Akauliza, "Hawa watu pamoja nawe ni kinanani?" Yakobo akasema,
Ni watoto ambao Mungu amempa mtumishi wako kwa neema." [6] Kisha wajakazi
wakakaribia pamoja na watoto wao, nao wakasujudia. [7] Akafuata Lea pia na watoto
wake wakaja na kusujudia. Mwisho Yusufu na Raheli wakaja na kusujudia. [8] Esau
akasema, Unamaanisha nini kwa makundi haya yote niliyokutana nayo?" Yakobo
akasema, "Kutafuta kibali mbele za bwana wangu. [9] Esau akasema, "Ninayo ya
kutosha, ndugu yangu. Tunza uliyonayo kwa ajili yako mwenyewe." [10] Yakobo
akasema, "Hapana, tafadhari, ikiwa nimeona kibali mbele zako, basi upokee zawadi
yangu kutoka mkononi mwangu, na ni kama kuona uso wa Mungu, na umenipokea.
[11] Tafadhari pokea zawadi yangu uliyoletewa, kwa sababu Mungu amenitendea kwa
neema, na kwa sababu ninavyo vya kutosha." Hivyo Yakobo akamsihi, na Esau
akamkubali. [12] Kisha Esau akasema, "Haya na tuondoke. Nitakutangulia." [13] Yakobo
akamwambia, "Bwana wangu anajua kwamba watoto ni wadogo, na kwamba kondoo
na ng'ombe wananyonyesha ndama wao. Ikiwa watapelekwa kwa haraka hata siku
moja, wanyama wote watakufa. [14] Tafadhari bwana wangu na amtangulie mtumishi
wake. Nitasafiri polopole, kwa kadili ya mifugo iliyo mbele yangu, na kadili ya watoto,
hata nitakapofika kwa bwana wangu huko Seiri." [15] Esau akasema, haya nikuachie
baadhi ya watu wangu waliopamoja nami." Yakobo akasema, "Kwa nini kufanya
hivyo? Bwana wangu amekuwa mkalimu kwangu kiasi cha kutosha." [16] Hivyo Esau
akaanza kurudi Seiri. [17] Yakobo akasafiri kuelekea Sukothi, akajijengea nyumba,
na akafanya mazizi kwa ajili ya mifugo wake. Hivyo jina la eneo linaitwa Sukothi.
[18] Yakobo alipokuja kutoka Padani Aramu, akafika salama katika mji wa Shekemu,
uliyo katika nchi ya Kanaani. Akapiga kambi karibu na mji. [19] Kisha akanunu sehemu
ya ardhi alipokuwa ameweka hema yake kutoka kwa wana wa Hamori, baba wa
Shekemu, kwa vipande mia vya fedha. [20] Akajenga madhabahu pale na kuiita El
Elohe Israeli.

# 34

[1] Basi Dina, Binti wa Lea aliyemzalia Yakobo, akaenda kuwaona wasichana wa
nchi. [2] Shekemu mwana wa Hamori Mhivi, mwana mfalme wa nchi, akamwona
na akamkamata kwa nguvu na kulala naye. [3] Akavutiwa na Dina, binti Yakobo.
Akampenda msichana na kuongea naye kwa upole. [4] Shekemu akamwambia Hamori
baba yeke, kusema, "Nipe msichana huyu kuwa mke wangu." [5] Basi Yakobo akasikia

kwamba alikuwa amemchafua Dina binti yake. Wanawe walikuwa pamoja na
wanyama uwandani, hivyo Yakaobo akawangoja hata walipokuja. 6 Hamori baba
wa Shekemu akaenda kuongea na Yakobo. 7 Wana wa Yakobo waliposikia neno
hili wakaja kutoka uwandani. Watu hawa walichukizwa sana. Walikasirika sana
kwa sababu alikuwa amemwaibisha Israeli kwa kumlazimisha binti wa Yakobo, kwa
maana jambo kama hilo halikupasa kutendeka. 8 Hamori akaongea nao, akisema,
“Shekemu mwanangu anampenda binti yenu. Tafadhari mpeni kuwa mke wake.
9 Mwoane nasi, tupeni binti zenu, na mjichukulie binti zetu kwa ajili yenu wenyewe.
10 Mtaishi nasi, na nchi itakuwa wazi kwa ajili yenu kufanya biashara humo, na
kupata mali.” 11 Shekemu akamwambia baba yake na ndugu zake, “Na nione kibari
machoni penu, na chochote mtakachoniambia nitatoa. 12 Niambieni kiasi kikubwa
chochote cha mahari na zawadi kama mtakavyo, nami nitatoa chochote msemacho,
lakini mnipe msichana kuwa mke wangu.” 13 Wana wa Yakobo wakamjibu Shekemu
na Hamori baba yake kwa hila, kwa sababu Shekemu alikuwa amemnajisi Dina
dada yao. 14 Wakawambia, “Hatuwezi kufanya jambo hili, kumpa dada yetu
mtu yeyote ambaye hajatailiwa; kwani hiyo ni aibu kwetu. 15 Kwa sharti hili
peke yake tutakubaliana nanyi: iwapo mtatailiwa kama sisi, ikiwa kila mtu mme
miongoni mwenu atatailiwa. 16 Ndipo tutakapowapa binti zetu, nasi tutachukua
binti zenu kwetu sisi wenyewe, na tutaishi nanyi na kuwa wamoja. 17 Lakini
kama hamtusikilizi na kutailiwa, ndipo tutakapomchukua dada yetu na kuondoka.
18 Maneno yao yakawafurahisha Hamori na Shekemu mwanaye. 19 Kijana hakukawia
kufanya walichokisema, kwa maana alipendezwa na binti Yakobo, na kwa sababu
alikuwa mtu aliyeheshimiwa sana katika nyumba ya babaye. 20 Hamori na Shekemu
mwanaye wakaenda katika lango la mji wao na kuongea na watu wa mji, kusema,
21 “Watu hawa wanaamani nasi, hivyo na waishi katika nchi na kufanya biashara
humo kwa maana, kweli, nchi ni kubwa ya kuwatosha. Haya na tuwachukue binti zao
kuwa wake, nasi tuwape binti zetu. 22 Kwa shariti hili pekee watu hawa wanakubali
kuishi nasi na kuwa wamoja: ikiwa kila mwanamme miongoni mwetu atatailiwa,
kama wao. 23 Je wanyama wao na vitu vyao - wanyama wao wote kuwa wetu? Haya
na tukubaliane nao, nao wataishi kati yetu.” 24 Watu wote wa mji wakamsikiliza
Hamori na Shekemu, mwanaye. Kila mwanamme akatailiwa. 25 Katika siku ya tatu,
walipokuwa katika maumivu bado, wawili wa wana wa Yakobo (Simoni na Lawi,
kaka zake Dina), wakachukua kila mmoja upanga wake na kuushambulia mji ambao
ulikuwa na uhakika wa ulinzi wake, nao wakauwa wanamme wote. 26 Wakamwua
Hamori na Shekemu kwa makali ya upanga. Wakamchukua Dina kutoka nyumba
ya Shekemu na kuondoka. 27 Wale wana wengine wa Yakobo wakaja kwa maiti
na kuuteka nyara mji, kwa sababu watu wale walikuwa wamemnajisi dada yao.
28 Wakachukua makundi yao ya kondoo, mbuzi, punda, na kila kitu ndani ya mji
na viunga vyake 29 utajiri wote. Watoto na wake zao wote, wakawachukua. Hata
wakachukua kila kitu kilichokua katika nyumba. 30 Yakobo akawambia Simoni na
Lawi, “Mmeleta shida juu yangu, kunifanya ninuke kwa wenyeji wa nchi, Wakanaani
na Waperizi. Mimi nina watu wachache. Ikiwa watajikusanya pamoja kinyume
changu na kunishambulia.” 31 Lakini Simoni na Lawi wakasema, “Je Shekemu
alipaswa kumtendea dada yetu kama kahaba?”

## 35

1 Mungu akamwambia Yakobo, “Inuka, panda kwenda Betheli, na ukae pale.
Unijengee madhabahu pale, niliyekutokea pale ulipomkimbia Esau kaka yako.”
2 Kisha Yakobo akawambia nyumba yake na wote aliokuwa nao, “Wekeni mbali
miungu yote ya kigeni iliyo kati yenu, jitakaseni wenyewe, na kubadili mavazi

yenu. 3 Kisha tuondoke na kwenda Betheli. Nitajenga pale madhabahu kwa
Mungu, aliyenijibu katika siku ya shida yangu, naye amekuwa pamoja nami kila
nilikokwenda. 4 Hivyo wakampa Yakobo miungu yote ya kigeni iliyokuwa mikononi
mwao, na heleni zilizokuwa katika masikio yao. Yakobo akazifukia chini ya mwaloni
uliokuwa karibu na Shekemu. 5 Kwa kadili walivyo safiri, Mungu akaifanya miji yote
iliyokuwa karibu nao kuhofu, hivyo watu hao hawakuwafuatia wana wa Yakobo.
6 Hivyo Yakobo akafika Luzu(ndiyo Betheli), ulioko katika nchi ya Kanaani, yeye
na watu wote aliokuwa nao. 7 Alijenge madhabahu na kuliita eneo hilo El Betheli,
kwa sababu Mungu alikuwa amejifunua kwake, alipokuwa akimkimbia ndugu yake.
8 Debora, mlezi wa Rebeka, akafa. Akazikwa chini kutoka Betheli chini ya mwaloni,
hivyo ikaitwa Aloni Bakuthi. 9 Yakobo alipokuja kutoka Padani Aramu, Mungu
akamtokea tena na kumbariki. 10 Mungu akamwambia, “Jina lako ni Yakobo, lakini
jina lako halitakuwa Yakobo tena. Jina lako litakuwa Israeli.” Hivyo Mungu akamwita
jina lake Israeli. 11 Mungu akamwambia, “Mimi ni Mungu Mwenyezi, Uwe mwenye
kuzaa na kuongezeka. Taifa na wingi wa mataifa watakujia, na wafalme watatoka
miongoni mwa uzao wako. 12 Nchi ambayo nilimpa Ibrahimu na Isaka, nitakupa
wewe. Nami nitaupa pia uzao wako baada yako nchi hii.” 13 Mungu akapanda
kutoka mahali alipoongea naye. 14 Yakobo akaweka nguzo katika eneo ambalo Mungu
alikuwa ameongea naye, nguzo ya jiwe. Akamimina juu yake sadaka ya kinywaji
na akamimina mafuta juu yake. 15 Yakobo akaiita sehemu Mungu aliyoongea naye,
Betheli 16 Wakaendelea na safari kutoka Betheli. Walipokuwa kitambo kabla ya
kufika Efrathi, Raheli akashikwa na uchungu. 17 Akawa na utungu mzito. Alipokuwa
katika utungu mzito zaidi, mkunga akamwambia, “Usiogope, kwani sasa utapata
mtoto mwingine wa kiume.” 18 Hata alipokaribia kufa, kwa pumzi yake ya mwisho
akamwita jina lake Benoni, lakini baba yake akamwita jina lake Benjamini. 19 Raheli
akafa na kuzikwa katika njia iendayo Efrathi (ndio Bethlehemu). 20 Yakobo akaweka
nguzo katika kaburi lake. Ndiyo alama ya kaburi la Raheli hata leo. 21 Israeli
akaendelea na safari na akaweka hema yake kuvuka mnara wa walinzi wa kondoo.
22 Yakobo alipokuwa akiishi katika nchi hiyo, Rubeni akalala na Bilha suria wa
baba yake, na Israeli akasikia kuhusu hilo. Basi Yakobo alikuwa na wana kumi na
mbili. 23 Wanawe kwa Lea walikuwa Rubeni, mzaliwa wa kwanza wa Yakobo, na
Simoni, Lawi, Yuda, Isakari, na Zabuloni. 24 Wanawe kwa Raheli walikuwa Yusufu
na Benjamini. 25 Wanawe kwa Bilha, mjakazi wa Raheli walikuwa Dani na Naftali.
26 Wana wa Zilpa, mjakazi wa Lea, walikuwa Gadi na Asheri. Hawa wote walikuwa
wana wa Yakobo waliozaliwa kwake huko Padani Aramu. 27 Yakobo akaja kwa
Isaka, baba yake, huko Mamre katika Kiriathi Arba (jina sawa na Hebroni), alipoishi
Ibrahimu na Isaka. 28 Isaka akaishi miaka mia moja na themanini. 29 Isaka akapumua
pumzi yake ya mwisho na akafa, na akakusanywa kwa wahenga wake, na mtu mzee
amejaa siku. Esau na Yakobo, wanawe, wakamzika.

## 36

1 Hivi ndivyo vizazi vya Esau (aliyeitwa pia Edom). 2 Esau akachukua wakeze
kutoka kwa Wakanaani. Hawa walikuwa wake zake: Ada binti Eloni Mhiti;
Oholibama binti Ana, mjukuu wa Zibeoni Mhivi; na 3 Basemathi, binti Ishmaeli,
dada wa Nebayothi. 4 Ada akamzaa Elifazi kwa Esau, na Basemathi akamzaa Reueli.
5 Oholibama akamzaa Yeushi, Yalamu, na Kora. Hawa walikuwa wana wa Esau
waliozaliwa kwake katika nchi ya Kananaani. 6 Esau akawachukua wakeze, wanawe,
binti zake, na watu wote wa nyumba yake, mifugo wake - wanyama wake wote, na
mali yake yote, aliyokuwa amekusanya katika nchi ya Kanaani, na akaenda katika
nchi iliyoko mbali kutoka kwa Yakobo nduguye. 7 Alifanya hivi kwa sababu mali zao

zilikuwa nyingi sana kwa wao kuishi pamoja. Nchi waliyokuwa wamekaa isingeweza
kuwafaa kwa mifugo yao. 8 Hivyo Esau, aliyejulikana pia kama Edomu, akakaa katika
nchi ya kilima Seiri. 9 Hivi ndivyo vizazi vya Esau, babu wa Waedomu katika nchi
ya mlima Seiri. 10 Haya yalikuwa majina ya wana wa Esau: Elifazi mwana wa
Ada, mkewe Esau; Reueli mwana wa Basemathi, mkewe Esau. 11 Wana wa Elifazi
walikuwa Temani, Omari, Zefo, Gatamu, na Kenazi. 12 Timna, suria wa Elifazi, mwana
wa Esau, akamzaa Amaleki. Hawa walikuwa wajukuu wa Ada, mkewe Esau. 13 Hawa
walikuwa wana wa Reueli: Nahathi, Zera, Shama, na Miza. Hawa walikuwa wajukuu
wa Basemathi, mkewe Esau. 14 Hawa walikuwa wana wa Oholibama, mkewe Esau,
aliyekuwa binti Ana na mjukuu wa Zibeoni. Alimzalia Esau Yeushi, Yalamu, na Kora.
15 Hizi zilikuwa koo kati ya vizazi vya Esau: uzao wa Elifazi, mzaliwa wa kwanza
wa Esau: Temani, Omari, Zefo, Kenazi, Kora, 16 Gatamu, na Amaleki. Hivi vilikuwa
vizazi vya koo kutoka kwa Elifazi katika nchi ya Edomu. Walikuwa wajukuu wa Ada.
17 Hizi zilikuwa koo kutoka kwa Reueli, mwana wa Esau: Nahathi, Zera, Shama, Miza.
Hizi zilikuwa koo kutoka kwa Reueli katika nchi ya Edomu. Walikuwa wajukuu wa
Basemathi, mkewe Esau. 18 Hizi zilikuwa koo za Oholibama, mkewe Esau: Yeushi,
Yalamu, Kora. Hizi ni koo zilizotoka kwa Oholibama mkewe Esau, binti Ana. 19 Hawa
walikuwa wana wa Esau na koo zao. 20 Hawa walikuwa wana wa Seiri Mhori, wenyeji
wa nchi hiyo: Lotani, Shobali, Zibeoni, Ana, 21 Dishoni, Ezeri, na Dishani. Hizi
zilikuwa koo the Wahori, wenyeji wa Seiri katika nchi ya Edomu. 22 Wana wa Lotani
walikuwa Hori na Hemani, na Timna alikuwa dada wa Lotani. 23 Hawa walikuwa
wana wa Shobali: Alvani, Manahathi, Ebali, Shefo, na Onamu. 24 Hawa walikuwa
wana wa Zibeoni: Aia na Ana. Huyu ndiye Ana aliyeona chemichemi za moto nyikani,
alipokuwa akichunga punda wa Zibeoni babaye. 25 Hawa walikuwa watoto wa Ana:
Dishoni na Oholibama, binti Ana. 26 Hawa walikuwa wana wa Dishoni: Hemdani,
Eshbani, Ithrani, na Kerani. 27 Hawa walikuwa wana wa Ezeri: Bilhani, Zaavani,
na Akani. 28 Hawa walikuwa wana wa Dishani: Uzi na Arani. 29 Hizi zilikuwa
koo za Wahori: Lotani, Shobali, Zibeoni, na Ana, 30 Dishoni, Ezeri, Dishani: hizi
zilikuwa koo za Wahori, kulingana na ukoo ulivyoorodheshwa katika nchi ya Seiri.
31 Hawa walikuwa wafalme waliomiliki katika nchi ya Edomu kabla ya mfalme yeyote
kumilika juu ya Waisraeli: 32 Bela mwana wa Beori, alitawala huko Edomu, na jina la
mji wake lilikuwa Dinhaba. 33 Bela alipofariki, kisha Yobabu mwana wa Zera kutoka
Bozra, akatawala mahali pake. 34 Yobabu alipofariki, Hushamu aliyekuwa wa nchi
ya Watemani, akatawala mahali pake. 35 Hushamu alipofariki, Hadadi mwana wa
Bedadi aliyewashinda Wamidiani katika nchi ya Moabu, akatawala mahali pake. Jina
la mji wake lilikuwa Avithi. 36 Hadadi alipofariki, kisha Samla wa Masreka akatawala
mahali pake. 37 Samla alipofariki, kisha Shauli wa Rehobothi kando ya mto alitawala
mahali pake. 38 Shauli alipofariki, kisha Baali Hanani mwana wa Akbori akatawala
mahali pake. 39 Baali Hanani mwana wa Akbori, alipokufa, kisha Hadari akatawala
mahali pake. Jina la mji wake lilikuwa Pau. Jina la mkewe lilikuwa Mehetabeli, binti
Matredi, mjukuu wa Me Zahabu. 40 Haya ndiyo yalikuwa majina ya wakuu wa koo
kutoka uzao wa Esau, kwa kufuata koo zao na maeneo yao, kwa majina yao: Timna,
Alva, Yethethi, 41 Oholibama, Ela, Pinoni, 42 Kenazi, Temani, Mbza, 43 Magdieli, na
Iramu. Hawa walikuwa wakuu wa ukoo wa Edomu, kwa kufuata makao yao katika
nchi waliyomiliki. Nao ni Esau, baba wa Waedomu.

# 37

1 Yakobo akaishi katika nchi aliyokaa babaye, katika nchi ya Kanaani. 2 Haya
ndiyo matukio yaliyomhusu Yakobo. Yusufu, aliyekuwa kijana wa miaka kumi
na saba, alikuwa akilichunga kundi pamoja na ndugu zake. Alikuwa pamoja
na wana wa Bilha na pamoja na wana wa Zilpa, wake wa baba yake. Yusufu

akaleta taarifa yao mbaya kwa baba yao. [3] Basi Israeli akampenda Yusufu kuliko
wanawe wote kwa sababu alikuwa mwana wa uzee wake. Akamshonea vazi
zuri. [4] Ndugu zake wakaona kwamba baba yao alimpenda sana kuliko ndugu
zake wote. Wakamchukia na hawakuongea naye vema. [5] Yusufu akaota ndoto, na
akawambia ndugu zake. Wakamchukia zaidi. [6] Aliwambia, “Tafadhari sikilizeni
ndoto hii niliyoiota. [7] Tazama, tulikuwa tukifunga miganda ya nafaka shambani
na tazama, mganda wangu ukainuka na kusimama wima, na tazama, miganda
yenu ikasogea na kuuinamia mganda wangu” [8] Ndugu zake wakamwambia, “Je ni
kweli utatutawala? Je utatutawala juu yetu? Hata wakamchukia zaidi kwa ajili
ya ndoto zake na maneno yake. [9] Akaota ndoto nyingine na kuwasimulia ndugu
zake. Alisema, “Tazama, nimeota ndoto nyingine: Jua na mwezi na nyota kumi
na moja ziliniinamia.” [10] Akamwambia baba yake vile vile alivyowambia ndugu
zake, na baba yake akamkemea. Akamwambia, Je umeota ndoto ya namna gani
hii? Je mama yako na mimi na ndugu zako kweli tutakuja kukuinamia mpaka
chini?” [11] Ndugu zake wakamwonea wivu, lakini baba yake akaliwema jambo hilo
moyoni. [12] Ndugu zake wakaenda kulichunga kundi la baba yao huko Shekemu.
[13] Israeli akamwambia Yusufu, 'Je ndugu zako hawalichungi kundi huko Shekemu?
Njoo, nami nitakutuma kwao.” Yusufu akamwambia, “nipo tayari.” [14] Akamwambia,
“Basi nenda, uwaone ndugu zako na kundi wanaendeleaje, na uniletee neno.” Hivyo
Yakobo akamtuma kutoka katika bonde la Hebroni, na Yusufu akaenda Shekemu.
[15] Mtu mmoja akamwona Yusufu. Tazama, Yusufu alikuwa akizunguka kondeni. Yule
mtu akamwuliza, “Unatafuta nini?” [16] Yusufu akamwambia, “Nawatafuta ndugu
zangu. Tafadhari, niambie, wananalichunga wapi kundi.” [17] Yule mtu akasema,
“Waliondoka mahali hapa, kwa maana niliwasikia wakisema, 'Haya twende Dothani.”
Yusufu akawafuata ndugu zake na kuwaona huko Dothani. [18] Wakamwona kutokea
mbali, na kabla hajawakaribia, wakapanga njama ya kumwua. [19] Ndugu zake
wakaambiana wao kwa wao, “Tazama, mwotaji anakaribia. [20] Njoni sasa, na tumwue
na kumtupa katika mojawapo ya mashimo haya. Nasi tutasema, 'Mnyama mkali
amemrarua.' Nasi tutaona ndoto zake zitakuwaje.” [21] Rubeni alilisikia hilo na
kumwokoa kutoka katika mikono yao. Alisema, “Tusiuondoe uhai wake.” [22] Rubeni
aliwambia, “Msimwage damu. Mtupeni katika shimo hili lililopo nyikani, lakini
msiweke mikono yenu juu yake” - ili kwamba aweze kumwokoa katika mikono yao
na kumrudisha kwa baba yake. [23] Ikawa Yusufu alipowafikia ndugu zake, walimvua
vazi lake zuri. [24] Wakamchukua na kumtupa shimoni. Shimo lilikuwa tupu bila
maji. [25] Wakakaa chini kula mkate. Walipoinua macho yao na kuangalia, na,
tazama, msafara wa Waishmaeli ulikuwa ukija kutoka Gileadi, pamoja na ngamia
wao waliochukua viungo, malhamu na manemane. Walikuwa wakisafiri kuvichukua
kuelekea Misri. [26] Yuda akawambia ndugu zake, “Ni faida gani kama tutamwua
ndugu yetu na kufunika damu yake? [27] Haya, na tumwuze kwa Waishmaeli na
wala tusiweke mikono yetu juu yake. Kwani yeye ni ndugu yetu, nyama yetu.”
Ndugu zake wakamsikiliza. [28] Wafanyabiashara wa Kimidiani wakapita. Ndugu
zake wakamwinua na kumtoa Yusufu shimoni. Wakamwuza Yusufu kwa Waishmaeli
kwa vipande ishirini vya fedha. Waishmaeli wakamchukua Yusufu mpaka Misri.
[29] Rubeni akarudi kwenye shimo, na, tazama, Yusufu hakuwemo shimoni. Akararua
mavazi yake. [30] Akarudi kwa ndugu zake na kusema, “Kijana yuko wapi? Na
mimi, je niende wapi?” [31] Wakachinja mbuzi na kisha wakalichukua vazi la Yusufu
na kulichovya katika damu. [32] Kisha wakalipeleka kwa baba yao na kusema,
“Tumeiona hii. Tafadhari angalia kwamba ni vazi la mwanao au hapana.” [33] “Yakobo
akaitambua na kusema, “Ni nguo ya mwanangu. Mnyama wa mwitu amemrarua.
Bila shaka Yusufu ameraruliwa katika vipande. [34] Yakobo akararua mavazi yake na

kuvaa mavazi ya magunia katika viuno vyake. Akaomboleza kwa ajili ya mwanawe
siku nyingi. 35 Wanawe na binti zake wote wakainuka na kumfariji, lakini alikataa
kufarijiwa. Akasema, "Hakika nitashuka kuzimu nikimwombolezea mwanangu."
Babaye akamlilia. 36 Wamidiani wakamwuza huko Misri kwa Potifa, afisa wa Farao,
kepteni wa walinzi.

# 38

1 Ikawa wakati ule Yuda akawaacha ndugu zake na kukaa na Mwadulami fulani,
jina lake Hira. 2 Pale akakutana na binti Mkanaani jina lake Shua. Akamwoa na kulala
naye. 3 Akawa mjamzito na kuzaa mwana. Akaitwa Eri. 4 Akawa mjamzito tena na
kuzaa mwana tena. Akamwita jina lake Onani. 5 Akazaa mwana mwingine akamwita
jina lake Shela. Alikuwa huko Kezibu alipomzaa. 6 Yuda akaona mke kwa ajili ya Eri,
mzaliwa wake wa kwanza. Jina lake Tamari. 7 Eri, mzaliwa wa kwanza wa Yuda,
alikuwa mwovu mbele za Yahwe. Yahwe akamwua. 8 Yuda akamwambia Onani,
"Lala na mke wa nduguyo. Fanya wajibu wa shemeji kwake, na umwinulie nduguyo
mwana." 9 Onani alijua kwamba mtoto asingekuwa wake. Pindi alipolala na mke
wa kaka yake, alimwaga mbegu juu ya ardhi ili kwamba asimpatie nduguye mtoto.
10 Alilolifanya lilikuwa ovu mbele za Yahwe. Yahwe akamwua pia. 11 Kisha Yuda
akamwambia Tamari, mkwewe, "Ukakae mjane katika nyumb aya baba yako hadi
Shela, mwanangu, atakapokuwa." Kwani aliogopa, "Asije akafa pia, kama nduguze."
Tamari akaondoka na kuishi katika nyumba ya babaye. 12 Baada ya muda mrefu, binti
Shua, mkewe Yuda, alikufa. Yuda akafarijika na kwenda kwa wakatao kondoo wake
manyoya huko Timna, yeye na rafiki yake, Hira Mwadulami. 13 Tamari akaambiwa,
"Tazama, mkweo anakwenda Timna kukata kondoo wake manyoya." 14 Akavua
mavazi yake ya ujane na akajifunika kwa ushungi. Akakaa katika lango la Enaimu,
lililoko kando ya njia iendayo Timna. Kwa maana aliona kwamba Shela amekua
lakini akupewe kuwa mke wake. 15 Yuda alipomwona alidhani ni kahaba kwa maana
alikuwa amefunika uso wake. 16 Akamwendea kando ya njia na kusema, "Njoo,
tafadhari uniruhusu kulala nawe" - kwani hakujua kwamba alikuwa ni mkwewe -
naye akasema, "Utanipa nini ili ulale nami? 17 Akasema, "Nitakuletea mwana mbuzu
wa kundi." Akasema, "Je utanipa rehani hata utakapo leta?" 18 Akasema, "Nikupe
rehani gani?" Naye akasema, "Mhuri wako na mshipi, na fimbo iliyo mkononi
mwako." Akampa na kulala naye. Akawa mjamzito. 19 Akaamka na kuondoka.
Akavua ushungi wake na kuvaa vazi la ujane wake. 20 Yuda akatuma mwana mbuzi
kutoka kundini kwa mkono wa rafiki yake Mwadulami ili aichukue rehani kutoka
katika mkono wa mwanamke, lakini hakumwona. 21 Kisha Mwadulami akauliza watu
wa sehemu hiyo,"Yupo wapi kahaba aliyekuwa Enaimu kando ya njia?" Wakasema,
hapajawai tokea kahaba hapa." 22 Akarudi kwa Yuda na kusema, "Sikumwona. Pia
watu wa eneo hilo wamesema, 'Hajawai kuwapo kahaba hapa." 23 Yuda akasema,
"Mwache akae na vitu, tusije tukaaibika. Hakika, nimemletea mwanambuzi, lakini
hukumwona." 24 Ikawa baada ya miezi mitatu Yuda akaambiwa, "Tamari mkweo
amefanya ukahaba, na kwa hakika, yeye ni mjamzito." Yuda akasema, "Mleteni hapa
ili achomwe." 25 Alipoletwa nje, alipeleka ujumbe kwa mkwewe, "Mimi ni mjamzito
kwa mtu mwenye vitu hivi." Akasema, "Tambua tafadhari, mhuri huu na mshipi
na fimbo ni vya nani." 26 Yuda akavitambua na kusema, "Yeye ni mwenye haki
kuliko mimi, kwani sikumpa Shela, mwanangu awe mme wake." Hakulala naye tena.
27 Muda wake wa kujifungua ukafika, tazama, mapacha walikuwa tumboni mwake.
28 Ikawa alipokuwa akijifungua mmoja akatoa mkono nje, na mkunga akachukua
kitambaa cha rangi ya zambarau na kukifunga katika mkono wake na kusema, "Huyu
ametoka wa kwanza." 29 Ikawa aliporudisha mkono wake, tazama, ndugu yake

akatoka kwanza. Mkunga akasema, “Umetokaje” Na akaitwa Peresi. 30 Kisha ndugu
yake akatoka, akiwa na utepe wa zambarau juu ya mkono wake, naye akaitwa Zera.

## 39

1 Yusufu akaletwa Misri. Potifa, aliyekuwa afisa wa Farao mkuu wa walinzi
na Mmisri, akamnunua kutoka kwa Waishmaeli, waliokuwa wamempeleka pale.
2 Yahwe alikuwa pamoja na Yusufu na akawa mtu aliyefanikiwa. Aliishi katika
nyumba ya Mmisri bwana wake. 3 Bwana wake akaona kwamba Yahwe alikuwa
pamoja naye na kwamba Yahwe alifanikisha kila kitu alichokifanya. 4 Yusufu akapata
kibali mbele zake. Akamtumikia Potifa. Potifa akamfanya msimamizi juu ya nyumba
yake, na kila alichokimiliki, akakiweka chini ya uangalizi wake. 5 Ikawa alipomfanya
msimamizi juu ya nyumba yake na juu ya kila kitu alichomiliki, Yahwe akaibariki
nyumba ya Mmisri kwa sababu ya Yusufu. Baraka za Yahwe zilikuwa juu ya kila kitu
alichokuwa nacho Potifa nyumbani na shambani. 6 Potifa akaweka kila alichokuwa
nacho chini ya uangalizi wa Yusufu. Hakuwa na haja ya kufikiri juu ya lolote
isipokuwa chakula alichokula tu. Basi Yusufu alikuwa kijana mzuri na wa kuvutia.
7 Ikawa baada ya hayo mke wa bwana wake akamtamani Yusufu. Akamwambia,
“Lala nami.” 8 Lakini yeye alikataa na kumwambia mke wa bwana wake, “Tazama,
bwana wangu haangalii chochote nikifanyacho nyumbani, na ameweka kila kitu
anachokimiliki chini ya uangalizi wangu. 9 Hakuna mtu aliye mkuu katika nyumba
hii kuliko mimi. Hajanidhuiria chochote isipokuwa wewe, kwa sababu wewe ni
mkewe. Ni kwa namna gani basi naweza kufanya uovu mkuu namna hii na kumtenda
dhambi Mungu? 10 Akamwambia Yusufu siku baada ya siku, lakini yeye akakataa
kulala naye wala kuwa naye. 11 Ikawa siku moja aliingia ndani kufanya kazi yake.
Hakuna mtu yeyote wa nyumbani aliyekuwepo pale ndani. 12 Akashika nguo zake na
kusema, “Lala nami.” Akaacha nguo zake mikononi mwake, akakimbia, na kutoka
nje. 13 Ikawa, alipoona kwamba ameziacha nguo zake mikononi mwake na kwamba
amekimbia nje, 14 akawaita watu wa nyumbani mwake na kuwambia, “Tazama,
Potifa ameleta Mwebrania huyu kutudhihaki. Aliingia kulala nami, na nikapiga
kelele. 15 Ikawa aliponisikia nikipiga kelele, akaniacha na nguo yake, akakimbia,
na kutoka nje.” 16 Akaweka nguo zake karibu naye hata bwana yake alipokuja
nyumbani. 17 Akamwambia maelelezo haya, “Yule mtumishi Mwebrania uliyemleta
kwetu, aliingia kunidhihaki. 18 Ikawa nilipopiga kelele, akaacha nguo yake kwangu
akakimbia nje.” 19 Ikawa, bwana wake aliposikia maelezo aliyoambiwa na mkewe,
“Hivi ndivyo mtumishi wako alivyonitenda,” alikasirika sana. 20 Bwana wa Yusufu
akamchukua na kumweka gerezani, mahali walipowekwa wafungwa wa mfalme.
Akawa pale kifungoni. 21 Lakini Yahwe alikuwa pamoja na Yusufu na kumwonyesha
uaminifu wa agano. Akampa kibali mbele ya mlinzi wa gereza. 22 Mlinzi wa gereza
akawaweka mikononi mwa Yusufu wafungwa wote waliokuwa gerezani. Chochote
walichokifanya, kilikuwa chini ya uangalizi wa Yusufu. 23 Mlinzi wa gereza hakuwa
na wasiwasi juu ya chochote kilichokuwa mkononi mwake, kwa sababu Yahwe
alikuwa pamoja naye. Yahwe akafanikisha kila alichokifanya.

## 40

1 Ikawa baada ya mambo haya, mnyweshaji wa mfalme wa Misri na mwokaji wa
mfalime walimkosa bwana wao, mfalme wa Misri. 2 Farao akawakasirikia hawa
maafsa wawili, mkuu wa wanyweshaji na mkuu wa waokaji. 3 Akawaweka katika
lindo katika nyumba ya kapteni wa walinzi, katika gereza lile Yusufu alimofungwa.
4 Kapteni wa walinzi akamweka Yusufu kuwa mtumishi wao. Walikaa kifungoni
kwa muda fulani. 5 Wote wakaota ndoto - mnyweshaji na mwokaji wa mfalme wa

Misri waliokuwa wamefungwa gerezani - kila mmoja akaota ndoto usiku huo huo,
na kila ndoto ilikuwa na tafsiri yake. 6 Yusufu akaja kwao asubuhi na kuwaona.
Tazama, walikuwa na uzuni. 7 Akawauliza maafsa wa Farao waliokuwa pamoja
naye kifungoni katika nyumba ya bwana wake, kusema, “Kwa nini leo mnaoneka
wenye uzuni?” 8 Wakamwambia, Sisi wote tumeota ndoto na hakuna wakuitafsiri.”
Yusufu akawambia, “Je tafsiri haitoki kwa Mungu? Niambieni, tafadhari.” 9 Mkuu wa
wanyweshaji akamwambia Yusufu ndoto yake. Akamwambia, “Katika ndoto yangu,
tazama, kulikuwa na mzabibu mbele yangu. 10 Na kulikuwa na matawi matatu
katika mzabibu huo. Ulipochipua, ukachanua maua na kuzaa vichala vya zabibu.
11 Kikombe cha Farao kilikuwa mkononi mwangu. Nikachukua zabibu na kuzikamua
katika kikombe cha Farao, na kukiweka kikombe katika mkono wa Farao.” 12 Yusufu
akamwambia, “Tafsiri yake ni hii. Yale matawi matatu ni siku tatu. 13 Ndani ya siku
tatu Farao atakiinua kichwa chako na kukurudisha katika nafasi yako. Utakiweka
kikombe cha Farao katika mkono wake, kama ulivyokuwa ulipokuwa mnyweshaji
wake. 14 Lakini unikumbuke ukifanikiwa, na unionesha wema. Unitaje kwa Farao
na kuniondoa hapa gerezani. 15 Maana hakika nilitekwa kutoka katika nchi ya
Waebrania. Na hapa sijafanya chochote kinachonipasa niwekwe gerezani.” 16 Mkuu
wa waokaji alipoona kwamba tafsiri ilikuwa ya kuvutia, akamwambia Yusufu, “Mimi
pia niliota ndoto, na tazama, vikapu vitatu vya mikate vilikuwa juu ya kichwa
changu. 17 Katika kikapu cha juu kulikuwa na kila aina za bidhaa ya kuokwa kwa
Farao, lakini ndege wakavila ndani ya kikapu juu ya kichwa changu.” 18 Yusufu
akajibu na kusema, “Tafsiri ni hii. Vikapu vitatu ni siku tatu. 19 Ndani ya siku tatu
Fareao atakiinua kichwa chako kutoka kwako na atakutundika juu ya mtu. Ndege
watakula mwili wako.” 20 Ikawa siku ya tatu ambayo ilikuwa ni siku ya kuzaliwa
kwa Farao. Akafanya sherehe kwa watumishi wake wote. “Akakiinua juu” kichwa
cha mkuu wa wanyweshaji na kichwa cha mkuu wa waokaji, kati ya watumishi
wake. 21 Akamrudisha mkuu wa wanyweshaji katika majukumu yake, na akakiweka
tena kikombe katika mkono wa Farao. 22 Lakini akamtundika mkuu wa waokaji,
kama Yusufu alivyokuwa amewatafsiria. 23 Hata hivyo mkuu wa wanyweshaji
hakukumbuka kumsaidia Yusufu. Badala yake, alimsahau.

# 41

1 Ikawa mwishoni mwa miaka miwili mizima Farao akaota ndoto. 2 Tazama,
alikuwa amesimama kando ya Nile. Tazama, ng'ombe saba wakatoka katika mto
Nile, wakupendeza na wanene, na wakajilisha katika nyasi. 3 Tazama, ng'ombe
wengine saba wakatoka katika Nile baada yao, wasiopendeza na wamekondeana.
Wakasimama ukingoni mwa mto kando ya wale ng'ombe wengine. 4 Kisha wale
ng'ombe wasiopendeza na waliokonda wakawala wale waliokuwa wanapendeza na
walionenepa. 5 Kisha Farao akaamka. Kisha akalala na kuota mara ya pili. Tazama,
masuke saba ya nafaka yalichipua katika mche mmoja, mema na mazuri. 6 Tazama,
masuke saba, membamba na yaliyokaushwa na upepo wa mashariki, yakachipua
baada yake. 7 Masuke membamba yakayameza yale masuke saba mema yote. Farao
akaamka, na, tazama, ilikuwa ni ndoto tu. 8 Ikawa wakati wa asubuhi roho yake
ikafadhaika. Akatuma na kuwaita waganga na wenye hekima wote wa Misri. Farao
akawasimlia ndoto zake, lakini hakuna aliyeweza kumtafsiria Farao. 9 Kisha mkuu
wa wanyweshaji akamwambia Farao, “Leo ninayafikiri makosa yangu. 10 Farao
aliwakasirikia watumishi wake, na kutuweka kifungoni katika nyumba ya kapteni
wa walinzi, mkuu wa waokaji na mimi. 11 Tuliota ndoto usiku huo mmoja, yeye
na mimi. Kila mmoja aliota kwa kadili ya tafsiri yake. 12 Pamoja nasi kulikuwa na
kijana Mwebrania, mtumishi wa kapteni wa walinzi. Tulimwambia na akatutafsiria

ndoto zetu. Alitutafsiria kila mmoja wetu kulingana na ndoto yake. 13 Ikawa
kama alivyotutafsiria, ndivyo ilivyokuwa. Farao alinirudisha katika nafasi yangu,
lakini akamtundika yule mwingine." 14 Ndipo Farao alipotuma na kumwita Yusufu.
Kwa haraka wakamtoa gerezani. Akajinyoa mwenyewe, akabadili mavazi yake, na
akaingia kwa Farao. 15 Farao akamwambia Yusufu, "Nimeoda ndoto, lakini hakuna
wa kuitafsiri. Lakini nimesikia kuhusu wewe, kwamba unaposikia ndoto unaweza
kuitafsiri." 16 Yusufu akamjibu Farao, kusema, "Siyo katika mimi. Mungu atamjibu
Farao kwa uhakika." 17 Farao akamwambia Yusufu, "Katika ndoto yangu, tazama,
nilisimama katika ukingo wa Nile. 18 Tazama, ng'ombe saba wakatoka ndani ya
Nile, wanene na wakuvutia, nao wakajilisha katika nyasi. 19 Tazama, ng'ombe
wengine saba wakapanda baada yao, dhaifu, wabaya, na wembaba. Sijawao kuona
wabaya kama hao katika nchi yote ya Misri. 20 Wale ng'ombe wembamba na wabaya
wakawala wale ng'ombe saba na wanene. 21 Walipokuwa wamemaliza kuwala wote,
haikujulikana kama walikuwa wamewala, kwani walibaki wabaya kama mwanzo.
Kisha nikaamka. 22 Niliona katika ndoto yangu, na tazama, masuke saba yakatoka
katika bua moja, jema na limejaa. 23 Tazama, masuke saba zaidi, yaliyonyauka,
membamba na yamekaushwa na upepo wa mashariki, yakachipua baada yake.
24 Yale masuke membamba yakayameza masuke saba mema. Niliwaambia waganga
ndoto hizi, lakini hakuna aliyeweza kunielezea." 25 Yusufu akamwambia Farao,
"Ndoto za Farao ni moja. Mungu amemwambia Farao kuhusu jambo analokwenda
kulifanya. 26 Wale ng'ombe saba wema ni miaka saba, na masuke saba mema ni
miaka saba. Ndoto ni moja. 27 Na wale ng'ombe saba wembamba na wabaya
waliokuja baadaye ni miaka saba, na pia masuke saba membamba yaliyokaushwa
na upepo wa mashariki itakuwa miaka saba ya njaa. 28 Hilo ni jambo nililomwambia
Farao. Mungu amemfunulia Farao jambo analokwenda kulifanya. 29 Tazama, miaka
saba yenye utele mwingi inakuja katika nchi yote ya Misri. 30 Na miaka saba ya njaa
itakuja baada yake, na utele wote katika nchi ya Misri utasahaulika, na njaa itaiaribu
nchi. 31 Utele hautakumbukwa katika nchi kwa sababu ya njaa itakayofuata, kwa
kuwa itakuwa kali sana. 32 Kwamb ndoto ilijirudia kwa Farao sababu ni kwamba
jambo hili limeanzishwa na Mungu, na Mungu atalitimiza hivi karibuni. 33 Basi Farao
atafute mtu mwenye maharifa na busara, na kumweka juu ya nchi ya Misri. 34 Farao
na afanye hivi: achague wasimamizi juu ya nchi. Na wachukue sehemu ya tano ya
mazao ya Misri katika miaka saba ya shibe. 35 Na wakusanye chakula chote cha hii
miaka myema ijayo na kuitunza nafaka chini ya mamlaka ya Farao, kwa chakula
kutumika katika miji. Wakiifadhi. 36 Chakula kitakuwa matumizi ya nchi kwa miaka
saba ya njaa itakayokuwa katika nchi ya Misri. Kwa njia hii nchi haitaaribiwa na
njaa." 37 Ushauri huu ukawa mwema machoni pa Farao na machoni pa watumishi
wake wote. 38 Farao akawambia watumishi wake, "Je tunaweza kumpata mtu kama
huyu, ambaye ndani yake kuna Roho wa Mungu?" 39 Hivyo Farao akamwambia
Yusufu, "Kwa vile Mungu amekuonesha yote haya, hakuna mtu mwenye ufahamu na
busara kama wewe. 40 Utakuwa juu ya nyumba yangu, watu wangu watatawaliwa
kwa kadili ya neno lako. Katika kiti cha enzi peke yake mimi nitakuwa mkuu
kuliko wewe." 41 Farao akamwambia Yusufu, "Tazama, nimekuweka juu ya nchi
yote ya Misri." 42 Farao akavua pete yake ya mhuri kutoka katika mkono wake na
kuiweka katika mkono wa Yusufu. Akamvika kwa mavazi ya kitani safi, na kuweka
mkufu wa dhahabu shingoni mwake. 43 Akataka apandishwe katika kibandawazi
cha pili alichokuwa nacho. Watu wakapiga kelele mbele yake, "Pigeni magoti."
Farao akamweka juu ya nchi yote ya Misri. 44 Farao akamwambia Yusufu, "Mimi
ni Farao, mbali na wewe, hakuna mtu atakayeinua mkono wake au mguu wake
katika nchi ya Misri." 45 Farao akamwita Yusufu jina la Zafenathi Panea." Akampa

Asenathi, binti wa Potifera kuhani wa On, kuwa mke wake. Yusufu akaenda juu ya
nchi yote ya Misri. 46 Yusufu alikuwa na umri wa miaka thelathini aliposimama
mbele ya Farao, mfalme wa Misri. Yusufu akatoka mbele ya Farao, na kwenda
katika nchi yote ya Misri. 47 Katika miaka saba ya shibe nchi ilipozaa kwa wingi.
48 Akakusanya chakula chote cha miaka saba iliyokuwako katika nchi ya Misri na
kukiweka chakula katika miji. Akaweka katika kila mji chakula cha mashamba
yaliyokizunguka. 49 Yusufu akahifadhi nafaka kama mchanga wa bahari, kingi kiasi
kwamba akaacha kuhesabu, kwa sababu kilikuwa hakihesabiki. 50 Kabla miaka
ya njaa kuingia Yusufu akapata wana wawili, ambao Asenathi, binti wa Potifera
kuhani wa On, alimzalia. 51 Yusufu akamwita mzaliwa wake wa kwanza Manase,
kwani alisema, “Mungu amenisahaurisha shida zangu zote na nyumba yote ya baba
yangu.” 52 Akamwita mwanawe wa pili Efraimu, kwani alisema, Mungu amenipa
uzao katika nchi ya mateso yangu.” 53 Miaka saba ya shibe iliyokuwa katika nchi
ya Misri ikafika mwisho. 54 Miaka saba ya njaa ikaanza, kama alivyokuwa amesema
Yusufu. Kulikuwa na njaa katika nchi zote, lakini katika nchi yote ya Misri kulikuwa
na chakula. 55 Nchi yote ya Misri ilipokuwa na njaa, watu wakapiga kelele kwa Farao
kwa ajili ya chakula. Farao akawambia Wamisri wote, “Nendeni kwa Yusufu na
mfanye atakavyosema.” 56 Njaa ilikuwa juu ya uso wote wa nchi. Yusufu akafungua
ghala zote na kuuza chakula kwa Wamisri. Njaa ilikuwa kali sana katika nchi ya
Misri. 57 Dunia yote ikaja Misri kununua nafaka kutoka kwa Yusufu, kwani njaa
ilikuwa kali katika dunia yote.

# 42

1 Basi Yakobo akafahamu kwamba kuna nafaka huko Misri. Akawambia wanawe,
“Kwa nini mnatazamana? 2 Akasema, “Tazama, nimesikia kwamba kuna nafaka
huko Misri. Shukeni huko mkatununulie chakula ili tuishi wala tusife.” 3 Ndugu
kumi wa Yusufu wakashuka Misri kununua chakula. 4 Lakini Benjamini, ndugu
wa Yusufu, Yakobo hakumtuma na ndugu zake, kwani alihofu kwamba madhara
yaweza kumpata. 5 Wana wa Israeli wakaja kununua miongoni mwao waliokuja,
kwani njaa ilikuwapo katika nchi ya Kanaani. 6 Basi Yusufu alikuwa mtawala
juu ya nchi. Ndiye aliyekuwa akiwauzia watu wote wa nchi. Ndugu zake
Yusufu wakaja na kumwinamia na nyuso zao hata chini. 7 Yusufu akawaona
ndugu zake na kuwatambua, lakini alijibadili kwao na kuongea nao kwa ukali.
Akawambia, “Mmetoka wapi?” Wakasema, “Kutoka nchi ya Kanaani ili kununua
chakula.” 8 Yusufu akawatambua ndugu zake, lakini wao hawakumtambua. 9 Yusufu
akazikumbuka ndoto aliyoziota kuhusu wao. Akawambia, “Ninyi ni wapelelezi.
Mmekuja kuona sehemu za nchi zisizolindwa.” 10 Wakamwambia, “Hapana, bwana
wangu. Watumishi wako wamekuja kununua chakula. 11 Sisi sote ni wana wa
baba mmoja. Ni watu wa kweli. Watumishi wako siyo wapelelezi.” 12 Akawambia,
“Hapana, mmekuja kuangalia sehemu za nchi zisizolindwa.” 13 Wakasema, “Sisi
watumishi wako tupo ndugu kumi na wawili, wana wa baba mmoja katika nchi
ya Kanaani. Tazama, mdogo yupo na baba yetu, na mwingine hayupo hai tena.”
14 Yusufu akawambia, “Ndivyo nilivyowambia; ninyi ni wapelelezi. 15 Mtajaribiwa
kwa njia hii. Kama aishivyo Farao, hamtaondoka hapa, mdogo wenu asipokuja hapa.
16 Mtumeni mmoja wenu amlete mdogo wenu. Mtabaki gerezani, hata maneno yenu
yatakapothibitishwa, kwamba kuna ukweli ndani yenu.” 17 Akawaweka kifungoni
kwa siku tatu. 18 Katika siku ya tatu Yusufu akaongea nao, “Fanyeni hivi nanyi
mtaishi, kwani ninamcha Mungu. 19 Kama ninyi ni watu wa kweli, mmoja wenu
atazuiliwa hapa gerezani, lakini ninyi nendeni, chukueni nafaka kwa ajili ya nyumba
zenu. 20 Mleteni mdogo wenu kwangu ili kwamba maneno yenu yathibitishwe

nanyi hamtakufa.” Wakafanya hivyo. 21 Wakasemezana wao kwa wao, “Kwa
kweli tuna hatia juu ya ndugu yetu kwani tuliona tabu ya nafsi yake alipotusihi
nasi hatukusikia. Kwa hiyo taabu hii imeturudia.” 22 Rubeni akawajibu, “Je
sikuwambia, 'Msitende dhambi juu ya kijana,' lakini hamkusikia? Basi, tazama,
damu yake inatakiwa juu yetu.” 23 Lakini hawakuja kwamba Yusufu anawaelewa,
kwani kulikuwa na mkalimani kati yao. 24 Akatoka kwao na kulia. Akarudi kwao
na kuongea nao. Akamchukua Simoni miongoni mwao na kumfunga mbele ya
macho yao. 25 Kisha Yusufu akaagiza watumishi kujaza mifuko yao kwa nafaka,
na kurudisha pesa ya kila mmoja katika gunia lake, nakuwapa mahitaji kwa safari.
Wakatendewa hivyo. 26 Hawa ndugu wakapandisha chakula chao juu ya punda zao
na kuondoka pale. 27 Mmoja wao alipofungua gunia lake ili kumlisha punda wao
katika sehemu waliyokuwa, akaona pesa yake. Tazama, ilikuwa mdomoni mwa gunia
lake. 28 Akawambia ndugu zake, “Pesa yangu imerudishwa. Tazama, imo katika
gunia langu.”Mioyo yao ikazimia na wakageukiana kila mmoja huku wakitetemeka.
Wakasema, “Ni nini hiki alichotutendea Mungu?” 29 Wakaenda kwa Yakobo, baba yao
katika nchi ya Kanaani na kumwambia yote yaliyowapata. 30 Wakasema, “Yule mtu,
bwana wa nchi, aliongea nasi kwa ukali na kutudhania kuwa wapelelezi katika nchi.
31 Tukamwambia, 'Tu watu wa kweli sisi. Sisi siyo wapelelezi. 32 Tupo ndugu kumi na
wawili, wana wa baba yetu. Mmoja hayupo hai tena, na mdogo yupo na baba yetu
katika nchi ya Kanaani.” 33 Yule mtu, bwana wa nchi, akatwambia, 'Kwa hili nitajua
kwamba ni watu wa kweli ninyi. Mwacheni mmojawapo wa ndugu zenu, chukueni
chakula kwa ajili ya njaa katika nyumba zenu, na mwondoke. 34 Mleteni mdogo
wenu kwangu. Ndipo nitakapojua kwamba ninyi si wapelelezi, lakini ni watu wa
kweli. Kisha nitamwachilia ndugu yenu, na mtafanya biashara katika nchi.” 35 Ikawa
walipoyafungua magunia yao, na tazama, kila mfuko wa fedha wa mmojawao
ulikuwa katika gunia lake. Wakati wao na baba yao walipoona mifuko yao ya fedha,
wakaogopa. 36 Yakobo baba yao akawambia, “Mmeniharibia watoto wao. Yusufu
hayupo hai tena, Simoni ameondoka, nanyi mmpeleke Benjamini naye. Mambo haya
yote ni kunyume changu.” 37 Rubeni akamwambia baba yake, kusema, “Unaweza
kuwaua wanangu wawili nisipomrudisha Benjamini kwako. Mweke mikononi
mwangu, nami nitamrudisha tena kwako.” 38 Yakobo akasema, “Mwanangu atashuka
pamoja nanyi. Kwani ndugu yake amekufa na yeye peke yake amebaki. Ikiwa
madhara yatampata katika njia mnayoiendea, ndipo mtakapozishusha mvi zangu
kaburini kwa huzuni.”

# 43

1 Njaa ilikuwa kali katika nchi. 2 Ikawa walipokuwa wametumia chakula chote
walichokitoa Misri, baba yao akawambia, “Nendeni tena; mtununulie chakula.”
3 Yuda akamwambia, “Yule mtu alituonya kwa ukali, 'Hamtauona uso wangu ndugu
yenu asipokuwa nanyi.' 4 Ikiwa utamtuma ndugu yetu pamoja nasi, tutashuka
na kuwanunulia chakula. 5 Lakini usipompeleka, hatutashuka. Kwa maana yule
mtu alitwambia, 'Hamtauona uso wangu ndugu yenu asipokuwa nanyi.” 6 Israeli
akawambia, “Kwa nini mlinitendea mimi vibaya hivyo kwa kumwambia mtu huyo
kwamba mnaye ndugu mwingine?” 7 Wakasema, “Yule mtu alituuliza habari zetu
na familia yetu kwa kina. Akasema, 'Je baba yenu bado yuko hai? Je mnaye
ndugu mwingine?'Tukamjibu kulingana na maswali haya. Tungejuaje kwamba
angetwambia, 'Mleteni ndugu yenu?” 8 Yuda akamwambia Israeli baba yake, “Mtume
kijana pamoja nami. Tutainuka na kwenda ili kwamba tuishi tusife, wote sisi, wewe,
na hata watoto wetu. 9 Mimi nitakuwa mdhamini wake. Utaniwajibisha mimi.
Kama nisipomleta na kumweka mbele yako, basi nibebe lawama daima. 10 Kwani

kama tusingekawia, bila shaka hata sasa tungekuwa tumekwisha rudi mara ya pili.”
[11] Israeli baba yao akawambia, “Kama ni hivyo, basi fanyeni hivi. Chukueni baadhi
ya mazao mazuri ya nchi katika mifuko yenu. Mchukulieni yule mtu zawadi: baadhi
ya malhamu, asali, viungo na manemane, jozi na lozi. [12] Chukueni pesa mara
mbili mikononi mwenu. Pesa iliyorudishwa katika magunia yenu, muichukue tena
katika mikono yenu. Pengine walikosea. [13] Mchukueni ndugu yenu pia. Inukeni na
mwende tena kwa mtu yule. [14] Mungu Mwenyezi na awape kuona rehema mbele ya
huyo mtu, hivyo kwamba awafungulie ndugu yenu mwingine na Benjamini. Kama
nikipotelewa na watoto, nimepotelewa.” [15] Watu wale wakachukua zawadi hii, na
katika mikono yao wakachukua mara mbili ya kiasi cha pesa, pamoja na Benjamini.
Wakaamka na kushuka Misri na kusimama mbele ya Yusufu. [16] Yusufu alipomwona
Benjamini akiwa nao, akamwambia mtunzaji wa nyumba yake, “Walete watu hao
ndani ya nyumba, chinja mnyama na umwandae, kwani watu hawa watakula
chakula cha mchana pamoja nami.” [17] Mtunzaji wa nyumba akafanya kama Yusufu
alivyosema. Akawaleta wale watu nyumbani kwa Yusufu. [18] Wale ndugu wakaogopa
kwa vile walivyoletwa katika nyumba ya Yusufu. Wakasema, “Ni kwa sababu ya
pesa iliyorudishwa katika magunia yetu mara ya kwanza tulipoletwa ndani, kwamba
atafute nafasi kinyume chetu. Kwamba aweze kutukamata na kutuchukua kama
watumwa, na kuchukua punda wetu.” Wakamsogelea mtunzaji wa nyumba ya
Yusufu, [19] nao wakaongea naye mlangoni mwa nyumba, [20] wakisema, “Bwana wangu,
tulikuja mara ya kwanza kununua chakula. [21] Ikawa, tulipofika katika eneo la
kupumzikia, tukafungua magunia yetu, na, tazama, pesa ya kila mtu ilikuwa katika
gunia lake, pesa yetu kwa kiasi kamili. Tumeileta katika mikono yetu. [22] Tumekuja
na pesa nyingine pia mikonon mwetu ili kununua chakula. Hatujui aliyeziweka
pesa katika magunia yetu.” [23] Mtunzaji wa nyumba akasema, “Amani iwe kwenu,
msiogope. Mungu wenu na Mungu wa baba yenu ndiye aliyeweka pesa katika
magunia yenu. Nilipokea pesa yenu.” Kisha mtunzaji wa nyumba akamleta Simoni
kwao. [24] Msimamizi wa nyumba akawapeleka watu hao katika nyumba ya Yusufu.
Akawapa maji, nao wakaosha miguu yao. Akawalisha punda wao. [25] Wakaandaa
zawadi kwa ajili ya Yusufu aliyekuwa akija mchana, kwani walikuwa wamesikia
kwamba watakula pale. [26] Yusufu alipokuja nyumbani, wakaleta nyumbani zawadi
iliyokuwa mikononi mwao, nao wakainama mbele yake hata chini. [27] Akawauliza
juu ya hali zao na kusema,”Je baba yenu hajambo, yule mzee mliyemnena? Je
bado yu hai?” [28] Wakasema, “Mtumishi wako baba yetu hajambo. Na bado yu
hai” Wakajinyenyekeza na kuinama chini. [29] Alipoinua macho yake akamwona
Benjamini ndugu yake, mwana wa mamaye, naye akasema, “Je huyu ndiye mdogo
wenu mliyemsema?” Na kisha akasema, “Mungu na awe mwenye neema kwako,
mwanangu.” [30] Yusufu akaharakisha kutoka chumbani, kwani aliguswa sana kuhusu
nduguye. Akatafuta mahali pa kulia. Akaingia chumbani mwake na kulia umo.
[31] Akaosha uso wake na kutoka nje. Akajizuia mwenyewe, akasema, “karibuni
chakula.” [32] Watumishi wakamhudumia Yusufu peke yake na wale ndugu peke yao.
Wamisri pale wakala pamoja naye peke yao kwa sababu Wamisri hawakuweza kula
mkate na Waebrania, kwani hilo ni chukizo kwa Wamisri. [33] Wale ndugu wakakaa
mbele yake, mzaliwa wa kwanza kwa kulingana na haki yake ya uzaliwa, na mdogo
kulingana na ujana wake. Wale watu wakashangaa wote. [34] Yusufu akapeleka
sehemu kwao kutoka katika chakula kilichokuwa mbele yake. Lakini sehemu ya
Benjamini ilikuwa mara tano zaidi ya kila ndugu zake. Wakanywa na wakamfurahia.

## 44

[1] Yusufu akamwamru msimamizi wa nyumba yake, akisema, “Jaza magunia ya

watu hawa kwa chakula, kiasi wawezacho kubeba, na uweke pesa ya kila mtu katika
mdomo wa gunia lake. 2 Uweke kikombe changu, cha fedha, katika mdomo wa
gunia la mdogo, na pesa yake ya chakula pia.” Msimamizi akafanya kama Yusufu
alivyosema. 3 Kukapambazuka asubuhi, na wale watu wakaruhusiwa kuondoka,
wao na punda zao. 4 Walipokuwa wametoka mjini lakini hawajafika mbali,
Yusufu akamwambia msimamizi wa nyumba yake, “Inuka, uwafuatie wale watu,
na utakapowapata, wambie, 'Kwa nini mmelipa uovu badala ya mema? 5 Je hiki siyo
kikombe ambacho bwana wangu hukinywea, na kikombe akitumiacho kwa uaguzi?
Mmefanya vibaya, kwa jambo hili mlilolifanya.” 6 Msimamizi wa nyumba akawapata
na kuwambia maneno haya. 7 Wakasema, “Kwa nini bwana wetu anasema maneno
kama haya? Na iwe mbali na watumishi wako kwamba wanaweza kufanya jambo
hili. 8 Tazama, pesa tulizozikuta katika midomo ya magunia yetu, tulizileta kwako
kutoka katika nchi ya Kanaani. Ni kwa jinsi gani basi tunaweza kuiba katika nyumba
ya bwana wako fedha au dhahabu? 9 Yeyote kitakayeonekana kwake miongoni
mwa watumishi wako, atakufa, nasi sote tutakuwa watumwa wa bwana wangu.”
10 Msimamizi akasema, “Basi na iwe kwa kadili ya maneno yenu. Yeye ambaye
kikombe kitaonekana kwake atakuwa mtumwa wangu, nanyi wengine mtakuwa bila
hatia.” 11 Kisha kila mtu akaharakisha na kulishusha gunia lake chini. na kila mtu
akalifungua gunia lake. 12 Msimamizi akatafuta. akaanza na mkubwa wa wote na
kumaliza kwa mdogo wa wote, na kikombe kikaonekana katika gunia la Benjamini.
13 Wakararua mavazi yao. Kila mtu akapakia juu ya punda wake nao wakarudi mjini.
14 Yuda na ndugu zake wakaja katika nyumba ya Yusufu. Bado alikuwepo pale, nao
wakainama mbele zake hata chini. 15 Yusufu akawambia, “Je ni nini hili mlilolifanya?
Je hamjui kwamba mtu kama mimi anafanya uaguzi. 16 Yuda akasema, “Je tunaweza
kumwambia nini bwana wangu? Tuseme nini? au ni jinsi gani twaweza kujithibitisha
wenyewe? Mungu ameona uovu wa watumishi wako. Tazama, sisi ni watumwa wa
bwana wangu, wote sisi na yule ambaye kikombe kimeonekana mkononi mwake.”
17 Yusufu akasema, “Na iwe mbali nami kwamba naweza kufanya hivyo. Mtu ambaye
kikombe kimeonekana mkononi mwake, huyu ndiye atakuwa mtumwa wangu, lakini
ninyi wengine, nendeni kwa amani kwa baba yenu.” 18 Ndipo Yuda alipomkaribia
na kusema, “Bwana wangu, tafadhari mwache mtumishi wako aseme neno katika
masikio ya bwana wangu, na usiziache hasira zako kuwaka dhidi ya mtumishi wako,
kwani wewe ni kama Farao. 19 Bwana wangu aliwauliza watumishi wake, kusema,
Je mnaye baba au ndugu?' 20 Nasi tukamwambia bwana wangu, 'Tunaye baba, ni
mzee, na mwana wa uzee wake, ni mdogo. Na ndugu yake alishakufa, na yeye peke
yake ndiye amebaki kwa mama yake, na baba yake anampenda.' 21 Nawe ukawambia
matumishi wako, 'Mleteni ili nimwone.' 22 Nasi tukamwambia bwana wangu, 'Kijana
hawezi kumwacha babaye. Kwani akimwacha babaye baba yake angekufa.' 23 Na
ukawambia watumishi wako, 'Mdogo wenu asipokuja pamoja nanyi, hamtauona
uso wangu tena.' 24 Na ikawa tulipokwenda kwa mtumishi wako baba yangu,
tulimwambia maneno ya bwana wangu. 25 Na baba yetu akasema, Nendeni tena,
mkatununulie chakula.' 26 Nasi tukasema, “Hatuwezi kushuka. Ikiwa mdogo wetu
atakuwa nasi, ndipo tutakaposhuka, kwani hatuwezi kuuona uso wa mtu yule mdogo
wetu asipokuwa pamoja nasi.' 27 Mtumishi wako baba yetu akatwambia, 'Mnajua
kwamba mke wangu alinizalia wana wawili. 28 Na mmoja akatoka kwangu nami
nikasema, “Bila shaka ameraruliwa vipande, na tangu hapo sijamwona.” 29 Nanyi
mkimchukua huyu naye kutoka kwangu mabaya yanaweza kumpata, mtashusha
mvi zangu kwa kaburini kwa huzuni. 30 Kwa hiyo, basi, nitapokuja kwa mtumishi
wako baba yangu, na kijana hayupo nasi, kwa kuwa uhai wake umefungamanishwa
katika uhai wa kijana, 31 itakuwa, atakapoona kwamba kijana hayupo nasi atakufa.

Na watumishi wako watazishusha mvi za mtumishi wako baba yetu kaburini kwa
masikitiko. 32 Kwani mtumishi wako alikuwa mdhamini wa kijana kwa baba yangu
na alisema, 'Ikiwa sitamleta kwako, ndipo nitakapokuwa mwenye hatia kwa baba
yangu daima." 33 Kwa hiyo sasa, tafadhari mwache mtumishi wake akae kama
mtumwa kwa bwana wangu badala ya kijana, na umwache kijana aende na ndugu
zake. 34 Kwa maana nitakwenda jinsi gani kwa baba yangu ikiwa kijana hayupo
nami? Ninaogopa kuona mabaya yatakayompata baba yangu."

# 45

1 Ndipo Yusufu hakuweza kujizuia mwenyewe mbele ya watumishi waliosimama
kando yake. Akasema kwa sauti, "Kila mtu aondoke." Hivyo hakuna mtumishi
aliyesimama kando yake wakati Yusufu alipojitambulisha kwa ndugu zake. 2 Akalia
kwa sauti, Wamisri wakasikia, na nyumba ya Farao wakasikia kuhusu hilo. 3 Yusufu
akawambia ndugu zake, "Mimi ni Yusufu. Je baba yangu ni mzima bado? Ndugu
zake hawakuweza kumjibu, kwani walitishwa na uwepo wake. 4 Kisha Yusufu
akawambia ndugu zake, "Nikaribieni, tafadhari." Nao wakasogea. Akawambia,
"Mimi ni Yusufu ndugu yenu, mliyemwuza Misri. 5 Lakini sasa msihuzunike au
kukasirika miongoni mwenu kwamba mliniuza huku, kwani Mungu alinituma mbele
yenu ili kutunza uhai. 6 Maana ni miaka miwili njaa imekuwa katika nchi, na
bado kuna miaka mitano ambayo hakutakuwa na kulima wala kuvuna. 7 Mungu
alinituma mbele yenu kuwahifadhi kama masalia duniani, na kuwaweka hai kwa
ukombozi mkuu. 8 Hivyo si ninyi mlionipeleka huku bali ni Mungu, na amenifanya
baba kwa Farao, bwana wa nyumba yake yote, na mtawala wa nchi yote ya Misri.
9 Fanyeni haraka mwende kwa baba yangu na mmwambie, 'Hivi ndivyo asemavyo
Yusufu mwanao, "Mungu amenifanya bwana kwa Wamisri wote. Shuka kwangu,
usikawie. 10 Utaishi katika nchi ya Gosheni, nawe utakuwa karibu nami, wewe na
watoto wako na watoto wa watoto wako, na kondoo wako na mbuzi wako, na yote
uliyonayo. 11 Nami nitakuhudumia pale, kwa maana bado kuna miaka mitano ya
njaa, hivyo usije ukaingia katika uhitaji, wewe, nyumba yako, na yote uliyonayo."
12 Tazama, macho yenu yanaona, na macho ya Benjamini ndugu yangu, kwamba ni
kinywa changu kinachoongea nanyi. 13 Mtamwambia baba yangu juu ya heshima
yangu yote huku Misri na yote mliyoyaona. Mtaharakisha na kumleta baba yangu
huku." 14 Akaikumbatia shingo ya Benjamini ndugu yake na kulia, na Benjamini
akalia shongoni mwake. 15 Akawabusu ndugu zake wote na kulia kwa ajili yao.
Baada ya hayo ndugu zake wakaongea naye. 16 Habari ya jambo hili ikasemwa
katika nyumba ya Farao: "Ndugu zake Yusufu wamekuja." Ikampendeza sana Farao
na watumishi wake. 17 Farao akamwambia Yusufu, "Wambie ndugu zako, 'Fanyeni
hivi: Wapakieni wanyama wenu na mwende katika nchi ya Kanaani. 18 Mchukueni
baba yenu na nyumba zenu mnijie. Nami nitawapa mema ya nchi ya Misri, nanyi
mtakula unono wa nchi.' 19 Basi mmeamriwa, 'Fanyeni hivi, chukueni mikokoteni
kutoka Misri kwa ajili ya watoto wenu na kwa ajili ya wake zenu. Mchukueni baba
yenu na kuja. 20 Msijari kuhusu mali zenu, kwani mema yote ya nchi ya Misri ni
yenu." 21 Wana wa Israeli wakafanya hivyo. Yusufu akawapa mikokoteni, kwa
kadili ya agizo la Farao, na akawapa mahitaji ya safari. 22 Akawapa wote mavazi
ya kubadilisha, lakini akampa Benjamini vipande mia tatu vya fedha na mavazi
matano ya kubadilisha. 23 Akampelekea baba yake: punda kumi waliobeba mema
ya Misri, punda majike kumi wamebeba nafaka, mikate, na mahitaji mengine kwa
baba yake kwa ajili ya safari. 24 Hivyo akawaruhusu ndugu zake nao wakaondoka.
Akawambia, "Angalieni msijemkagombana njiani." 25 Wakapanda kutoka Misri na
kuja katika nchi ya Kanaani, kwa Yakobo baba yao. 26 Wakamwambia "Yusufu bado

yu hai, na ndiye mtawala juu ya nchi yote ya Misri." Na moyo wake ulishikwa na
ushangao, kwani hakuwaamini. 27 Wakamwambia maneno yote ya Yusufu aliyokuwa
amewambia. Yakobo alipoona mikokoteni Yusufu aliyokuwa amepeleka kuwabeba,
roho ya Yakobo baba yao ikafufuka. 28 Israeli akasema, "Inatosha. Yusufu mwanangu
yu hai. Nitakwenda nikamwone kabla sijafa."

# 46

1 Israeli akasafiri na yote aliyokuwa nayo na akaja Beersheba. Pale akatoa sadaka
kwa Mungu wa Isaka baba yake. 2 Mungu akamwambia Israeli katika ndoto usiku,
akisema, "Yakobo, Yakobo." 3 Akasema, "Mimi hapa." Akasema, "Mimi ni Mungu,
Mungu wa baba yako. Usiogope kushuka Misri, kwa maana nitakufanya taifa kubwa
huko. 4 Nitakwenda pamoja nawe huko Misri, Nami nitakupandisha huku tena bila
shaka. Na Yusufu akayafunika macho yako kwa mikono wake." 5 Yakobo akainuka
kutoka Beersheba. Wana wa Israeli wakamsafirisha Yakobo baba yao, watoto wao,
na wake wao, katika mikokotene ambayo Farao alikuwa ameipeleka kuwachukua.
6 Wakachukua mifugo yao na mali zao walizokuwa wamezipata katika nchi ya
Kanaani. Wakaja Misri, Yakobo na uzao wake wote pamoja naye. 7 Akaja Misri
pamoja na wanawe na wana wa wanawe, binti zake na wana wa binti zake, na
uzao wake wote. 8 Haya ni majina ya watoto wa Israeli waliokuja Misri, Yakobo na
wanawe: Rubeni, mzaliwa wa kwanza wa Yakobo; 9 wana wa Rubeni Hanoki na Palu
na Hezroni na Karmi; 10 wana wa Simoni, Yemueli, Yamini, Ohadi, Yakini, Zohari,
na Shauli, wana wa mwanamke Mkanaani; 11 wana wa Lawi Gershoni, Kohathi, na
Merari. 12 Wana wa Yuda: Eri, Shela, Peresi, na Zera, (Lakini Eri na Onani walikufa
katika nchi ya Kanaani). Na wana wa Peresi walikuwa Hezroni na Hamuli. 13 Wana
wa Isakari walikuwa Tola, Puva, Lobu, na Shimroni; 14 Wana wa Zabuloni walikuwa
Seredi, Eloni, na Yahleeli 15 Hawa walikuwa wana wa Lea aliomzalia Yakobo huko
Padani Aramu, pamoja na na Dina binti yake. Wanawe na binti zake walikuwa
thelathini na watatu. 16 Wana wa Gadi walikuwa Zifioni, Hagi, Shuni, Ezboni, Eri,
Arodi, na Areli. 17 Wana wa Asheri walikuwa Imna, Ishva, Ishvi, na Beria; na Sera
alikuwa dada yao. Wana wa Beria walikuwa Heberi na Malkieli. 18 Hawa walikuwa
wana wa Zilpa, ambaye Labani alikuwa amempa Lea binti yake. Wana aliomzalia
Yakobo wote walikuwa kumi na sita. 19 Wana wa Raheli mkewe Yakobo walikuwa
Yusufu na Benjamini. 20 Huko Misri Manase na Efraimu walizaliwa kwa Yusufu
na Asenathi, binti Potifera kuhani wa Oni. 21 Wana wa Benjamini walikuwa Bela,
Bekeri, Ashbeli, Gera, Naamani, Ehi, Roshi, Mupimu, Hupimu, na Ardi. 22 Hawa
walikuwa wana wa Raheli waliozaliwa kwa Yakobo - jumla yao kumi na wanne.
23 Mwana wa Dani alikuwa Hushimu. 24 Wana wa Naftali walikuwa Yahzeeli, Guni,
Yezeri, na Shilemi. 25 Hawa walikuwa wana Bilha aliomzalia Yakobo, ambaye Labani
alimpa Raheli binti yake - wote walikuwa saba. 26 Wate waliokwenda na Yakobo,
waliokuwa uzao wake, bila kuhesabu wake wa wana wa Yakobo walikuwa sitini
na sita. 27 Pamoja na wana wawili wa Yusufu waliozaliwa kwake huko Misri,
watu wa familia yake waliokwenda Misri walikuwa sabini jumla yao. 28 Yakobo
akamtuma Yuda kuwatangulia mbele kwa Yusufu kuonesha njia mbele yake kwenda
Gosheni, nao wakaja katika eneo la Gosheni. 29 Yusufu akaandaa kibandawazi chake
na akaenda kumlaki baba yake huko Gosheni. Akamwona, akaikumbatia shingo
yake, na akalia shingoni mwake kwa kitambo. 30 Israeli akamwambia Yusufu, "Basi
na nife sasa, kwa kuwa nimeuona uso wako, kwamba bado uko hai." 31 Yusufu
akawambia ndungu zake na nyumba ya baba yake, "Nitakwenda na kumwambia
Farao, kusema, 'Ndugu zangu na nyumba ya baba yangu, waliokuwa katika nchi
ya Kanaani, wamenijia. 32 Watu hawa ni wafugaji, kwani wamekuwa watunza
wanyama. Wamekuja na makundi yao ya kondoo, na mbuzi, na vyote walivyonavyo.'

33 Itakuwa, Farao atakapowaita na kuwauliza, 'Kazi yenu ni ipi?' 34 mwambieni,
'Watumishi wako wamekuwa watunza wanyama tangu ujana wetu mpaka sasa, sisi,
na baba zetu.' Fanyeni hivyo ili mweze kuishi katika nchi ya Gosheni, kwani kila
mfugaji ni chukizo kwa Wamisri.”

# 47

1 Kisha Yusufu akaingia kwa Farao na kumwambia, “Baba yangu na ndugu zangu,
kondoo wao, mbuzi wao, na yote waliyonayo, wamefika kutoka katika nchi ya
Kanaani. Tazama, wapo katika nchi ya Gosheni.” 2 Akawachukua watano katika
ndugu zake na kuwatambulisha kwa Farao. 3 Farao akawambia ndugu zake, “Kazi
yenu ni nini?” Wakamwambia Farao, “Watumishi wako ni wafugaji, kama mababu
zetu.” 4 Kisha wakamwambia Farao, “Tumekuja kukaa kwa muda katika nchi.
Hakuna malisho kwa ajili ya makundi ya watumishi wako, kwa maana njaa ni
kali sana katika nchi ya Kanaani. Hivyo, tafadhari waache watumishi wako wakae
katika nchi ya Gosheni.” 5 Kisha Farao akamwambia Yusufu, kusema, “Baba yako
na ndugu zako wamekuja kwako. 6 Nchi ya Misri iko mbele yako. Mkalishe baba
yako na ndugu zako katika eneo zuri, nchi ya Gosheni. Ikiwa unafahamu watu
wenye uwezo miongoni mwao, uwaweke kuwatunza wanyama wangu.” 7 Kisha
Yusufu akamwingiza Yakobo baba yake na kumweka mbele ya Farao. Yakobo
akambariki Farao. 8 Farao akamwambia Yakobo, “Umeishi kwa muda gani?” 9 Yakobo
akamwambia Farao, “Miaka ya safari zangu ni mia moja na thelathini. Miaka
ya maisha yangu imekuwa mifupi na ya maumivu. Siyo kama miaka ya baba
zangu.” 10 Kisha Yakobo akambariki Farao na kuondoka mbele zake. 11 Kisha Yusufu
akamweka baba yake na ndugu zake. Akawapa eneo katika nchi ya Misri, sehemu
nzuri sana ya nchi, katika eneo la Ramesesi, kama Farao alivyokuwa ameagiza.
12 Yusufu akamhudumia baba yake kwa chakula, ndugu zake, na nyumba yote ya
baba yake, kulingana na hesabu ya wahitaji wao. 13 Basi hakukuwa na chakula
katika nchi yote; kwani njaa ilikuwa kali sana. Nchi ya Misri na nchi ya Kanaani
ikaharibika kwa sababu ya njaa. 14 Yusufu akakusanya pesa yote iliyokuwa katika
nchi ya Misri na nchi ya Kanaani, kwa kuwauzia wakaaji wake chakula. Kisha Yusufu
akaleta ile pesa katika kasri la Farao. 15 Pesa yote ya nchi za Misri na Kanaani
ilipokwisha, Wamisri wote wakaja kwa Yusufu wakisema, “Tupe chakula! Kwa nini
tufe mbele zako kwa maana pesa yetu imekwisha?” 16 Yusufu akasema, “Ikiwa pesa
yenu imekwisha, leteni wanyama wenu nami nitawapa chakula badala ya wanyama
wenu.” 17 Hivyo wakaleta wanyama wao kwa Yusufu. Yusufu akawapa chakula
kwa kubadilishana na farasi, kondoo, mbuzi na kwa punda. Akawalisha kwa mkate
kwa kubadilisha na wanyama wao mwaka ule. 18 Mwaka ule ulipokwisha, wakaja
kwake mwaka uliofuata na kumwambia, “Hatutaficha kwa bwana wangu kwamba
pesa yetu yote imekwisha, na wanyama ni wa bwana wangu. Hakuna kilichobaki
mbele za bwana wangu, isipokuwa miili yetu na nchi yetu. 19 Kwa nini tufe mbele
za macho yake, sisi na nchi yetu? Utununue sisi na nchi yetu badala ya chakula, na
sisi na nchi yetu tutakuwa watumishi wa Farao. Tupe mbegu ili kwamba tuishi na
tusife, na kwamba nchi isiwe tupu bila watu. 20 Hivyo Yusufu akamnunulia Farao
nchi yote ya Misri. Kwani kila Mmisri akauza shamba lake, kwa sababu njaa ilikuwa
kali sana. Kwa njia hii, nchi ikawa mali ya Farao. 21 Na watu, akawafanya kuwa
watumwa kutoka mpaka mmoja wa Misri hata mkapa mwingine. 22 Ilikuwa ni nchi
ya makuhani pekee ambayo Yusufu hakuinunua, kwa maana makuhani walikuwa
wakipewa posho. Walikula katika sehemu aliyowapa Farao. Kwa hiyo hawakuuza
nchi yao. 23 Kisha Yusufu akawambia watu, “Tazama, nimewanunua ninyi na nchi
yenu leo kwa ajili ya Farao. Basi mbegu hii hapa kwa ajili yenu, nanyi mtapanda

katika nchi. 24 Wakati wa mavuno, mtampa Farao sehemu ya tano, na sehemu
nne zitakuwa zenu, kwa mbegu za shamba na kwa chakula cha nyumba zenu na
watoto wenu." 25 Wakasema, "Umeokoa maisha yetu. Na tupate kibali machoni
pako. Tutakuwa watumishi wa Farao." 26 Hivyo Yusufu akaifanya kuwa sheria
inayofanya kazi hata leo katika nchi ya Misri, kwamba moja ya tano ni ya Farao. Eneo
la makuhani peke yake ndo halikufanywa kuwa la Farao. 27 Hivyo Israeli akaishi
katika nchi ya Misri, katika eneo la Gosheni. Watu wake wakapata umiliki pale.
Walikuwa wenye kuzaa na kuongezeka sana. 28 Yakobo akaishi katika nchi ya Misri
miaka kumi na saba, kwa hiyo miaka ya maisha ya Yakobo ilikuwa miaka mia moja
arobaini na saba. 29 Wakati wa kufa kwake Yakobo ulipokaribia, alimwita Yusufu
mwanaye na kumwambia, "Ikiwa nimepata kibali mbele zako, weka mkono wako
chini ya paja langu, na unitendee kwa uaminifu na kweli. Tafadhari usinizike Misri.
30 Nitakapolala na baba zangu, utanitoa Misri na kunizika katika eneo la kuzikia la
baba zangu." Yusufu akasema, "Nitafanya kama ulivyosema." 31 Israeli akasema,
"Niapie," na Yusufu akamwapia. Kisha Israeli akainama chini mbele ya kitanda
chake.

# 48

1 Ikawa baada ya mambo haya, mmojawapo akamwambia Yusufu, "Tazama,
baba yako ni mgonjwa." Hivyo akaondoka pamoja na wanawe wawili, Manase na
Efrahimu. 2 Yakobo alipoambiwa, "Tazama, mwanao Yusufu amekuja kukuona,"
Israeli akakusanya nguvu na kukaa juu ya kitanda. 3 Yakobo akamwambia Yusufu,
Mungu Mwenyezi alinitokea huko Luzu katika nchi ya Kanaani. Akanibariki na
4 kuniambia, 'Tazama, nitakupa uzao mwingi, na kukuzidisha. Nitakufanya kuwa
kusanyiko la mataifa. Nitakupa nchi hii wewe na uzao wako kuwa milki ya
milele.' 5 Na sasa wanao wawili, waliozaliwa kwako katika nchi ya Misri kabla
sijaja Misri, ni wangu. Efrahimu na Manase watakuwa wangu, kama walivyo
Rubeni na Simioni. 6 Watoto utakaowapata baada ya hapo ni wako; watahesabiwa
katika majina ya ndugu zao katika urithi wao. 7 Lakini kwangu mimi, nilipokuja
kutoka Padani, kwa uzuni yangu Raheli alikufa njiani katika nchi ya Kanaani,
wakati kungalipo kitambo kwenda Efrathi. Nilimzika pale katika njia iendayo
Efrathi" (ndio, Bethlehemu). 8 Israeli alipowaona wana wa Yusufu, akasema,
"Ni nani hawa?" 9 Yusufu akamwambia baba yake, "Hawa ni wanangu, Mungu
alionipa hapa:" Israeli akasema, "Walete kwangu, kwamba niwabariki." 10 Basi
macho ya Israeli yalikuwa yanashindwa kwa ajili ya umri wake, hivyo hakuweza
kuona. Hivyo Yusufu akawasogeza karibu yake, na akawabusu na kuwakumbatia.
11 Israeli akamwambia Yusufu, "Sikutazamia kuuona uso wako tena, Lakini Mungu
ameniruhusu kuwaona hata wanao." 12 Yusufu akawaondoa kati ya magoti ya Israeli,
na kisha akainama na uso wake juu ya nchi. 13 Yusufu akawachukua wote wawili,
Efrahimu katika mkono wake wa kulia kuelekea mkono wa kushoto wa Israeli,
na Manase katika mkono wake wa kulia kuelekea mkono wa kulia wa Israeli, na
akawasogeza kwake. 14 Israeli akainua mkono wake wa kulia na kuuweka juu ya
kichwa cha Efrahimu, aliyekuwa mdogo, na mkono wake wa kushoto juu ya kichwa
cha Manase. Akaipishanisha mikono yake, kwani Manase ndiye alikuwa mzaliwa
wa kwanza. 15 Israeli akambariki Yusufu, akisema, Mungu ambaye mbele zake
baba zangu Ibrahimu na Isaka walitembea, Mungu aliyenilinda hata leo, 16 malaika
walionilinda na madhara yote, awabariki vijana hawa. Jina langu na litajwe kwao,
na majina ya baba zangu Ibrahimu na Isaka. Na wawe makutano ya watu juu ya
nchi." 17 Yusufu alipoona baba yake ameweka mkono wake wa kulia juu ya kichwa
cha Efrahimu, haikumpendeza. Akauchukuwa mkono wa baba yake auweke katika

kichwa cha Manase. 18 Yusufu akamwambia baba yake, "Sivyo babangu; kwani huyu
ndiye mzaliwa wa kwanza. Uweke mkono wako juu ya kichwa chake." 19 Baba yake
akakataa na kusema, "Ninafahamu, mwanangu, nafahamu. Yeye naye atakuwa watu,
naye pia atakuwa mkuu. Lakini mdogo wake atakuwa mkuu kuliko yeye, na uzao
wake utakuwa wingi wa mataifa." 20 Israeli akawabariki siku hiyo kwa maneno haya,
"Watu wa Israeli watatamka baraka kwa majina yenu wakisema, Mungu na akufanye
kama Efrahimu na kama Manase'. "Kwa njia hii, Israeli akamweka Efrahimu mbele
ya Manase. 21 Israeli akamwambia Yusufu, "Tazama, ninakaribia kufa, lakini Mungu
atakuwa nanyi, na atawarudisha katika nchi ya baba zenu. 22 Kwako wewe, kwa
kuwa uko juu ya ndugu zako, ninakupa mtelemko wa mlima niliouchukuwa kutoka
kwa Waamori kwa upanga wangu na upinde wangu."

# 49

1 Kisha Yakobo akawaita wana wake, na kusema: "Jikusanyeni pamoja, ili
niwaambie yatakayowapata nyakati zijazo. 2 Kusanyikeni ninyi wenyewe na
msikilize, enyi wana wa Yakobo. Msikilizeni Israeli, baba yenu. 3 Reubeni, wewe ni
mzaliwa wangu wa kwanza, nguvu zangu, na mwanzo wa uwezo wangu, aliyesalia
katika heshima na nguvu. 4 Asiyezuilika kama maji yarukayo, hautakuwa na
umaharufu, kwa sababu ulikwenda juu ya kitanda cha baba yako. Hata ukakitia
unajisi; ulikipanda kwa kuvizia. 5 Simoni na Lawi ni ndugu. Panga zao ni silaha
za vurugu. 6 Ee nafsi yangu, usiingie barazani pao; usiingie katika mikutano yao,
kwani moyo wangu unaheshima kubwa kwa ajili yao. Kwani katika hasira yao
waliua watu. Iliwapendeza kuwakata visigino ng'ombe. 7 Hasira yao na ilaaniwe,
kwani ilikuwa kali - na ukali wao, kwani ulikuwa ni katili. Nitawagawa katika
Yakobo na kuwatawanya katika Israeli. 8 Yuda, ndugu zako watakusifu. Mkono
wako utakuwa shingoni mwa adui zako. Wana wa baba yako watainama mbele zako
9 Yuda ni mwana simba. Mwanangu, umetoka katika mawindo yako. Alisimama
chini, alijikunyata kama simba, kama simba jike. Je nana atakayejaribu kumwamsha?
10 Fimbo haitaondoka katika Yuda, wala fimbo ya utawala kutoka katika miguu
yake, hata atakapo kuja Shilo. Mataifa yatamtii. 11 Kumfunga punda wake kwenye
mzabibu, na mwanapunda wake katika mzabibu mzuri, amefua mavazi yake katika
divai, na kanzu yake katika damu ya vichala vya mzabibu. 12 Macho yake yatakuwa
mausi kama mvinyo, na meno yake meupe kama maziwa. 13 Zabuloni atakaa katika
fukwe ya bahari. Atakuwa bandari kwa ajili ya meli, na mpaka wake utakuwa hata
Sidoni. 14 Isakari ni punda mwenye nguvu, ajilazaye kati ya kondoo. 15 Anaona
mahali pazuri pa kupumzikia na nchi ya kupendeza. Atainamisha bega lake kwa
mzigo na kuwa mtumishi wake. 16 Dani atawaamua watu wake kama mojawapo ya
makabila ya Israeli. 17 Dani atakuwa nyoka kando ya njia, nyoka mwenye sumu
aumaye visigino vya farasi katika njia, hivyo aongozaye farasi huanguka nyuma.
18 Ninaungoja wokovu wako, Yahwe. 19 Gadi - wapanda farasi watamshambulia,
lakini yeye atawapiga katika visigino vyao. 20 Vyakula vya Asheri vitakuwa vingi,
naye ataandaa vyakula vya kifalme. 21 Naftali ni dubu jike asiyefungwa; atakuwa
na watoto wa dubu walio wazuri. 22 Yusufu ni tawi lizaalo, tawi lizaalo karibu na
kijito, ambaye matawi yake yako juu wa ukuta. 23 Mpiga mishale atamshambulia
na kumrushia na kumsumbua. 24 Lakini upinde wake utakuwa imara, na mikono
yake itakuwa hodari kwa sababu ya mikono ya Mwenyenguvu wa Yakobo, kwa ajili
ya jina la Mchungaji, Mwamba wa Israeli. 25 Mungu wa baba yako atakusaidia
na Mungu Mwenye enzi atakubariki kwa baraka mbinguni juu, baraka za vilindi
vilivyo chini, na baraka za maziwa na tumbo. 26 Baraka za baba yako ni kuu kuliko
baraka za milima ya zamani au vitu vilivyotamaniwa vya milima ya kale. Na viwe

katika kichwa cha Yusufu, hata juu ya taji ya kifalme kichwani pa ndugu zake.
27 Benjamini ni mbwamwitu mwenye njaa. Wakati wa asubuhi atalarua mawindo,
na jioni atagawa mateka.” 28 Haya ni makabila kumi na mbili ya Israeli. Hiki
ndicho baba yao alichowambia alipowabariki. Aliwabariki kila mmoja kwa baraka
iliyomstahili. 29 Kisha akawaelekeza na kuwaambia, “Ninakaribia kwenda kwa watu
wangu. Mnizike pamoja na babu zangu katika pango lililoko katika shamba la Efroni
Mhiti, 30 katika pango lililo katika shamba la Makpela, karibu na Mamre katika nchi
ya Kanaani, shamba Ibrahimu alilolinunua kwa Efron Mhiti kwa ajili ya eneo la
kuzikia. 31 Pale walimzika Ibrahimu na Sara mkewe; pale wakamzika Isaka na Rebeka
mkewe; na pale nikamzika Lea. 32 Shamba na pango lililomo lilinunuliwa kutoka kwa
watu wa Hethi.” 33 Yakobo alipomaliza maagizo hayo kwa wanawe, akaiweka miguu
yake kitandani, akakata roho, akawaendea watu wake

# 50

1 Yusufu akahuzunika sana hata akauangukia uso wa baba yake, akamlilia, na
kumbusu. 2 Yusufu akawaagiza watumishi wake matabibu kumtia dawa babaye.
Hivyo matabibu wakampaka dawa Israeli. 3 Wakatimiza siku arobain, kwani
huo ndio uliokuwa muda kamili wa kutia dawa. Wamisri wakamlilia kwa siku
sabini 4 Siku za maombolezo zilipotimia, Yusufu akaongea na watumishi wa baraza
la kifalme wa Farao kusema, “Ikiwa nimepata kibali machoni penu, tafadharini
ongeeni na Farao, kusema, 5 'Baba yangu aliniapisha, kusema, “Tazama, ninakaribia
kufa. Unizike katika kaburi nililolichimba kwa ajili yangu mwenyewe katika nchi
ya Kanaani. Ndipo utakaponizika.” Basi sasa niruhusu niende nimzike baba
yangu, na kisha nitarudi.” 6 Farao akajibu, “Nenda na umzika baba yako, kama
alivyokuwapisha.” 7 Yusufu akaenda kumzika baba yake. Maofisa wa Farao wote
wakaenda pamoja naye - washauri wa nyumba yake, maofisa waandamizi wote wa
nchi ya Misri, 8 pamoja na nyumba yote ya Yusufu na ndugu zake, na nyumba yote
ya baba yake. Lakini watoto wao, kondoo wao na makundi ya mbuzi wao yaliachwa
katika nchi ya Gosheni. 9 Vibandawazi na wapanda farasi pia walikwenda pamoja
naye. Lilikuwa kundi kubwa sana la watu. 10 Hata walipokuja katika sakafu ya
kupuria ya Atadi upande mwingine wa Yordani, wakaomboleza kwa majonzi ya
huzuni kubwa. Yusufu akafanya maombolezo ya siku saba kwa ajili ya babaye
pale. 11 Wenyeji wa nchi, Wakanaani, walipoona maombolezo katika sakafu ya Atadi,
wakasema, “Hili ni tukio la kuhuzunisha sana kwa Wamisri.” Ndiyo maana eneo hilo
likaitwa Abeli Mizraimu, lililoko mbele ya Yordani. 12 Hivyo wanawe wakamfanyia
Yakobo kama alivyokuwa amewaagiza. 13 Wana wake wakampeleka katika nchi
ya Kanaani na wakamzika katika pango katika shamba la Makpela, karibu na
Mamre. Ibrahimi alikuwa amelinunua pango pamoja na shamba kwa ajili ya eneo la
kuzikia. Alikuwa amelinunua kutoka kwa Efroni Mhiti. 14 Baada ya kuwa amemzika
babaye, Yusufu akarudi Misri, yeye, pamoja na ndugu zake, na wote waliokuwa
wamemsindikiza ili kumzika babaye. 15 Nduguze Yusufu walipoona kwamba baba
yao amekufa, wakasema, “Itakuwaje ikiwa Yusufu atatukasirikia na akataka kutulipa
kikamilifu kwa ajili ya uovu tuliomtenda?” 16 Hivyo wakamwagiza Yusufu, kusema,
“Baba yako alitoa maelekezo kabla hajafa, kusema, 17 'Mwambieni hivi Yusufu,
“Tafadhari samehe makosa ya ndugu zako na dhambi yao uovu waliokutenda.” Basi
wasamehe watumishi wa Mungu wa baba yako.” Yusufu akalia walipomwambia.
18 Ndugu zake pia wakaenda na kuinamisha nyuso zao mbele zake. Wakasema,
“Tazama, sisi ni watumishi wako.” 19 Lakini Yusufu akawajibu, “Msiogope, Je
mimi ni badala ya Mungu? 20 Lakini kwenu, mlikusudia kunidhuru, lakini Mungu
alikusudia mema, kuhifadhi maisha ya watu wengi, kama mwonavyo leo. 21 Hivyo

basi msiogope. Nitawahudumia ninyi na watoto wenu wadogo.” Kwa njia hii aliwatia
moyo na kuongea na mioyo yao kwa upole. [22] Yusufu akakaa Misri, pamoja na
familia ya baba yake. Akaishi miaka mia moja na kumi. [23] Yusufu akawaona
wana wa Efraimu hata kizazi cha tatu. Pia aliwaona wana wa Makiri mwana wa
Manase, waliowekwa katika magoti ya Yusufu. [24] Yusufu akawambia ndugu zake,
“Ninakaribia kufa; lakini kwa hakika Mungu atawajilia na kuwaongoza kutoka katika
nchi hii na kuwapeleka katika nch aliyoapa kumpa Ibrahimu, kwa Isaka na kwa
Yakobo.” [25] Kisha Yusufu akawaapisha watu wa Israeli kwa kiapo. Akasema, “Bila
shaka Mungu atawajilia. Wakati huo mtachukuwa mifupa yangu kutoka hapa.”
[26] Hivyo Yusufu akafa, mwenye miaka 110. Wakampaka dawa na akawekwa katika
jeneza huko Misri.

# Kutoka

1 Haya ndiyo majina ya wana wa Israeli waliokuja Misri pamoja na Yakobo kila
moja na familia yake: 2 Rubeni, Simioni, Lawi, na Yuda, 3 Isakari, Zebuluni, na
Benjamini, 4 Dani, Naftali, Gadi, na Asheri. 5 Jumla ya watu wa ukoo wa Yakobo
walikuwa sabini. Yusufu alikuwa Misri tayari. 6 Ndipo Yusufu, pamoja na kaka zake
wote, na kizazi chote wakafa. 7 Waisraeli walifanikiwa sana, wakaongezeka sana
idadi yao, na wakawa na nguvu maana nchi ilijazwa na wao. 8 Wakati huu sasa
mfalme mpya asiyemjua Yusufu aliinuka katika Misri. 9 Akawaambia watu wake,
“Tazama, hawa Waisraeli ni wengi na wenye nguvu kuliko sisi. 10 Njooni na tukae nao
kwa akili, ama sivyo wataendelea kuongezeka na kama vita ikiibuka, wataungana
na adui zetu, watapigana nasi, na kisha wataondoka.” 11 Hivyo wakawekea walinzi
ambao waliwatesa kwa kuwatumikisha kazi ngumu. Waisraeli walijenga maghala ya
miji kwa ajili ya Farao: Pishoni na Ramsei. 12 Lakini kadiri Wamisri walivyowatesa,
ndivyo Waisraeli waliendelea kuongezeka na kusambaa. Hivyo Wamisri wakaanza
kuwaogopa Waisraeli. 13 Wamisri waliwafanya Waisraeli wafanye kazi kwa nguvu
nyingi. 14 Waliyafanya maisha yao kuwa machungu kwa kuwafanyisha kazi ngumu
kwa vinu na matofali na kwa kila aina ya kazi za shambani. Kazi zao zote zilikuwa
ngumu. 15 Kisha mfalme wa Misri akawaambia wakunga wa Kiebrania; mmoja
wao aliitwa jina lake Shifra, na mwingine aliitwa Puha. 16 Akasema, “Wakati
mnapowasaidia wanawake wa Kiebrania wanapojifungua, chunguzeni wanapozaa.
Ikiwa ni mtoto wa kiume, basi muueni; bali ikiwa ni mtoto wa kike, basi mwacheni
aishi.” 17 Lakini wale Wakunga walimwogopa Mungu na hawakufanya kama mfalme
wa Misri alivyowaagiza; badala yake waliwaacha watoto wa kiume waishi. 18 Mfalme
wa Misri akawaita Wakunga na kuwaambia, “Kwanini mmefanya haya, na kuwaacha
watoto wa kiume wakaishi?” 19 Wale Wakunga wakamjibu Farao, “Hawa wanawake
wa Kiebrania siyo kama wanawake wa Kimisri. Hawa wana nguvu na jasiri sana
maana wao humaliza kuzaa kabla hata mkunga hajafika.” 20 Mungu aliwalinda hawa
Wakunga. Watu waliongezeka kwa idadi na kuwa na nguvu sana. 21 Kwa sababu
wale Wakunga walimwogopa Mungu, aliwapa familia. 22 Farao akawaagiza watu
wote, “Lazima mmutupe kila mtoto wa kiume anayezaliwa katika mto, lakini kila
mtoto wa kike wamwache aishi.”

## 2

1 Sasa mwanamme wa kabila la Lawi alimuoa mwanamke Mlawi. 2 Yule
mwanamke akapata mimba na kuzaa mtoto wa kiume. Alipoona ya kuwa alikuwa
mtoto mwenye afaya, alimficha kwa miezi mitatu. 3 Lakini alipokuwa hawezi
kuendelea kumficha tena, alichukua kikapu cha manyasi akakipaka sifa na lami.
Akamtia mtoto ndani yake na kukiweka juu ya maji katika majani kando ya mto.
4 Dada yake akasimama kwa mbali ili ajue yatakayompata. 5 Binti Farao akashuka
kuoga mtoni wakati vijakazi wake wakitembea kando ya mto. Naye akaona kile
kikapu katika majani na akamtuma kijakazi wake kwenda kukileta. 6 Alipokifungua,
aliomwona mtoto. Tazama, mtoto alikuwa analia. Alimhurumia na kusema, “Bila
shaka huyu ni mmoja wapo wa watoto wa Waebrania.” 7 Basi dada wa yule mtoto
akamwambia binti Farao, “Je naweza kwenda kukutafutia mwanamke wa Kiebrania
aje akulele mtoto kwa ajili yako?” 8 Binti Farao akamwambia, “Nenda.” Hivyo
yule binti akaenda na kumwita mama yake yule mtoto. 9 Binti Farao akamwambia
mama yake yule mtoto, “Mchukue mtoto huyu ukaninyonyeshee, nami nitakupa
posho.” Hivyo yule mwanamke akamchukua mtoto na kumnyonyesha. 10 Mtoto

alipokuwa mkubwa, akamleta kwa binti Farao, na akawa mtoto wake. Akamwita
jina lake Musa akisema, "Kwa sababu nilimtoa katika maji." 11 Musa alipokuwa
mtu mzima, alienda kwa watu wake na kuona kazi ngumu walizokuwa wanafanya.
Alimuona Mmisri akimpiga Mwebrania, mmoja wa watu wa jamii yake. 12 Aliangalia
huku na kule, na alipoona ya kuwa hakuna mtu, alimuua yule mmisri na kuuficha
mwili wake katika mchanga. 13 Alienda tena siku iliyofuata, na tazama, Waebrania
wawili walikuwa wanapigana. Alimwambia yule aliyekuwa na makosa, "Kwa
nini unampigia mwenzako?" 14 Lakini yule mtu alisema, "Ni nani aliyekuweka
wewe kuwa kiongozi na mwamuzi juu yetu? Unataka kuniua na mimi kama
ulivyomuua yule mmisri?" Ndipo Musa akaogopa na kusema, "Hakika niliyoyafanya
yamejulikana." 15 Farao aliposikia habari hizi, alijaribu kumuua Musa. Lakini Musa
alikimbia na kwenda kuishi katika nchi ya Wamidiani. Kule alikaa chini kando
ya mto. 16 Wakati huo kuhani wa Midiani alikuwa na mabinti saba. Walikuja
mtoni kuchota maji na kujaza vyombo vyao ili wawanyweshe mifuko ya baba yao.
17 Wachungaji walikuja na kutaka kuwafukuza, lakini Musa alienda kuwasaidia.
Kisha akawanywesha mifugo wao. 18 Wale mabinti walipoenda kwa Reueli baba yao,
aliwauliza, "Kwa nini mmerudi nyumbani mapema hivi leo?" 19 Wakamwambia,
"Mmisri mmoja alituokoa dhidi ya wachungaji. Pia alichota maji na kuwanywesha
mifugo wetu." 20 Kisha akawauliza binti zake, "Yu wapi sasa? Kwa nini mlimwacha?
Mwiteni ili apate kula chakula pamoja nasi." 21 Musa akakubali kukaa na yule mtu
ambaye pia alimpa binti yake Zipora ili amuoe. 22 Alizaa mtoto wa kiume, na Musa
akamwita jina lake Geshomu; akisema; "Nimekuwa mkazi katika nchi ya ugeni."
23 Muda mrefu baadaye, mfalme wa Misri akafa. Waisraeli walilalamika kwa sababu
ya kazi za utumwa. Walilia kutafuta msaada, na maombi yao yakamfikia Mungu
kwa sababu ya mateso yao. 24 Mungu aliposikia malalamiko yao, Mungu alikumbuka
agano lake na Abrahamu, na Isaka, na Yakobo. 25 Mungu aliwaona Waisraeli na
akaielewa hali yao.

# 3

1 Wakati huu Musa aliendelea kuchunga mifugo ya Yethro baba mkwe wake,
kuhani wa Midiani. Musa aliliongoza kundi la mifugo kuelekea upande wa mbali
wa jangwa mpaka kufika Horebu, mlima wa Mungu. 2 Akiwa pale malaika wa
Yahwe akamtokea kama mwali wa moto katika kichaka. Musa aliangalia, na tazama,
kichaka kiliwaka moto lakini hakikuteketea. 3 Musa akasema, "Nitageuka ili nione
kitaku hiki cha ajabu, kwa nini kichaka hakiteketei." 4 Yahwe alipoona ya kuwa
amegeuka upande ili aone, Mungu alimwita kutoka katika kile kichaka na kusema,
"Musa, Musa." Musa akasema, "Mimi hapa." 5 Mungu akasema, "Usinikaribie! Vua
viatu katika miguu yako, kwa kuwa mahali uliposimama ni mahali palipowekwa
wakfu kwa ajili yangu." 6 Aliongeza kusema, "Mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu
wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo." Kisha Musa akaufunika
uso wake, kwa kuwa aliogopa kumwangalia Mungu. 7 Yahwe akasema, "Hakika
nimeyaona mateso ya watu wangu walioko Misri. Nimesikia kelele zao kwa sababu
ya mabwana wao, kwa kuwa nayajua mateso yao. 8 Nimekuja chini kuwaokoa
dhidi ya mamlaka ya Wamisri na kuwatoa katika nchi ile na kuwaleta katika nchi
nzuri, pana, nchi ijaayo maziwa na asali; kwenye ukanda wa Wakanaani, Wahiti,
Waamori, Waperizi, Wahivi, na Wayebusi. 9 Sasa kilio cha watu wa Israeli kimenifikia
mimi. Zaidi sana, Mimi nimeyaona mateso ambayo Wamisri wanawatesa. 10 Sasa
basi, nitakutuma wewe kwa Farao ili upate kuwatoa watu wangu, wana wa Israeli,
kutoka katika nchi ya Misri." 11 Lakini Musa akamwambia Mungu, "Mimi ni nani
hata niende kwa Farao na kuwatoa Waisraeli kutoka Misri?" 12 Mungu akamjibu,

“Hakika nitakuwa pamoja nawe. Hii itakuwa ishara kwako ya kuwa nimekutuma.
Utakapokuwa umewatoa watu kutoka Misri, mtaniabubu mimi katika mlima huu.”
13 Musa akamwambia Mungu, “Nikienda kwa Waisraeli na kuwaambia, 'Mungu
wa baba zenu amenituma mimi kwenu,' na kisha wakiniambia, 'jina lake nani?'
nitawaambia nini?” 14 Mungu akamwambia Musa, “MIMI NIPO AMBAYE NIPO.”
Mungu akasema, “Ni lazima uwaambie Waisraeli, “MIMI NIPO amenituma kwenu.”
15 Pia Mungu akamwambia Musa, “Lazima uwaambie Waisraeli, 'Yahwe, Mungu wa
baba zenu, Mungu wa Abrahamu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo amenituma
mimi kwenu. Hili ndio jina langu milele, na hivi ndivyo nitakavyokumbukwa na
vizazi vyote.' 16 Nenda ukawakusanye wazee wa Israeli pamoja. Waambie, 'Yahwe,
Mungu wa baba zenu, Mungu wa Abrahamu, wa Isaka na Yakobo, amenitokea mimi
na kusema, “Hakika nimewatazama na nimeona yale mliyotendewa huko Misri.
17 Nimeahidi kuwatoa ninyi katika mateso ya Misri na kuwaleta katika nchi ya
Wakanaani, Wahiti, Wamwori, Waperizi, Wahivi, na Wayebusi. Nchi ijaayo maziwa
na asali.” 18 Watakusikiliza. Wewe pamoja na wazee wa Israeeli itawapasa kwenda
kwa mfalme wa Misri, na imewapasa kumwambia, 'Yahwe, Mungu wa Waebrania
amekutana nasi. Hivyo tuache sisi twende safari ya siku tatu katika jangwa ili tupate
kutoa sadaka kwa Yahwe Mungu wetu.' 19 Lakini nafahamu ya kuwa mfalme wa
Misri hatawaacha ninyi mwende, isipokuwa kwa kulazimishwa. 20 Nitainua mkono
wangu na kuwapiga Wamisri kwa miujiza yote nitakayoifanya kati yao. Baada ya
hayo, atawaacha mwende. 21 Nitawapa watu hawa kufadhiliwa kutoka kwa Wamisri
ili muondokapo msiende mikono mitupu. 22 Kila mwanamke ataomba kwa jirani
yake Mmisri na kwa kila mwanamke akaaye kwenye nyumba ya jirani yake, vyombo
vya fedha na vya dhahabu na nguo. Nanyi mtawavika watoto wenu wa kiume na
binti zenu. Kwa njia hii mtawateka nyara Wamisri.”

# 4

1 Musa akajibu, “Lakini itakuwaje wasiponiamini mimi au wasiponisikiliza na
kusema, 'Yahwe hajakutokea wewe?” 2 Yahwe akamwambia, “Hicho ni nini mkononi
mwako?” Musa aksema, “Ni fimbo.” 3 Yahwe akasema, “Itupe chini.” Musa akaitupa
chini ile fimbo, nayo ikageuka na kuwa nyoka. Musa akarudi nyumba. 4 Yahwe
akamwambia Musa, “Mchukue kwa kumshikia mkia wake.” Hivyo alimchukua yule
nyoka. Mara ikaggeuka na kuwa fimbo mkononi mwake tena. 5 “Hii ni ili wapate
kuamini ya kuwa Yahwe, Mungu wa baba zao, Mungu wa wa Abrahamu, Mungu
wa Isaka, na Mungu wa Yakobo amekutokea wewe.” 6 Yahwe pia alimwambia,
“Sasaingiza mkono wako ndani ya vazi lako.” Hivyo Musa akaingiza mkono wake
ndani ya vazi lake. Na alipoutoa nje, tazama, mkono wake ulikuwa na ukoma,
mweupe kama theluji. 7 Yahwe akasema, “Ingiza mkono wako ndani ya vazi
lako tena.” Hivyo akaingiza mkono wake ndani ya vazi lake, na alipoutoa nje
aliona ukiwa mzima tena kama ulivyo mwili wake wote. 8 Yahwe akasema, “Kama
hawatakuamini wewe - kama hawatazingatia ishara yanggu ya kwanza ya nguvu
zangu au kuziamini, basi wataamini ishara ya pili. 9 Na ikiwa hawataamini hata
ishara hizi zote mbili za nguvu zangu, au wasipokusikiliza wewe, basi chota maji
kutoka katika mto na uyamwage katika nchi kavu. Maji utakayoyamwaga yatakuwa
damu katika nchi kavu.” 10 Ndipo Musa akamwambia Yahwe, “Bwana, mimi ni
mzuri wa kuongea, si hapo kwanza au hata baada ya kuwa umeongea na mtumishi
wako. Mimi ni mdhaifu wa kuongea na nina kigugumizi.” 11 Yahwe akamwambia,
“Ni nani anayeumba mdomo wa mwanadamu? Ni nani amfanyaye mwanadamu
kuwa bubu au aone au kipofu? Je si mimi Yahwe? 12 Sasa nenda, nami nitauongoza
mdomo wako na nitakufundisha cha kusema.” 13 Lakini Musa akasema, “Bwana,

tafadhali mtume mtu mwingine, yeyote unayependa kumtuma.” 14 Kisha Yahwe
akamkasirikia Musa. Akasema, “Vipi kuhusu Aroni kaka yako yule Mlawi? Najua
ya kuwa anaweza kuongea vizuri. Hata hivyo, anakuja kukutana na wewe, na
atakapokuona moyo wake utajawa na furaha. 15 Wewe utaongea naye na utaweka
maneno ya kusema kinywani mwake. Nami nitakiongoza kinywa chako na kinywa
chake pia, nami nitaonesha ninyi nyote yawapasayo kutenda. 16 Yeye ataongea
na watu kwa niaba yako. Yeye atakuwa msemaji wako, na wewe utakuwa kama
Mungu kwake. 17 Utachukua hii fimbo pamoja nawe mkononi mwako. Kwa fimbo
hii utafanya ishara.” 18 Hivyo Musa alirudi kwa Yethro - baba mkwe wake na
kumwambia, “Niruhusu nipate kurudi kwa ndugu zangu walioko Misri ili niweze
kuona kama bado wako hai.” Yethro akwambia Musa, “Nenda kwa amani.” 19 Yahwe
akamwambia Musa kule Midiani, “Nenda, rudi Misri, kwa kuwa watu wote waliotaka
kukuua wameshakufa.” 20 Musa akamchukua mke wake na watoto wake wa kiume
na kuwapandisha kwenye punda. Akarudi mpaka nchi ya Misri, naye alichukua
fimbo ya Mungu pamoja naye mkononi mwake. 21 Yahwe akamwambia Musa,
“Utakaporudi Misri, jitahidi kufanya ishara zote nilizokupa kufanya mbele ya Farao.
Lakini nitaufanya moyo wake kuwa mgumu, naye hawatawaacha watu waende.
22 Lazima umwambie Farao, 'Hivi ndivyo asemavyo Yahwe: Israeli ni mtoto wangu,
mzaliwa wa kwanza wangu, 23 nami nakuamuru, “Mwache mwanangu aende ili
apate kuniabudu mimi.” Lakini kwa kuwa umekataa kumwachia, hakika nitamuua
mtoto wako wa kiume, mzaliwa wa kwanza wako.”' 24 Sasa wakiwa njiani, wakati
wa usiku walipopumzika, Yahwe alikutana na Musa na kutaka kumuua. 25 Kisha
Zipora akachukua kisu kikali na kukata govi la mtoto wake wa kiume na kuligusisha
miguuni pake. Kisha akasema, “Hakika wewe ni bwana harusi wangu kwa njia ya
damu.” 26 Hivyo Yahwe akamwachia. Akasema, “Wewe ni bwana harusi wa damu”
kwa sababu ya kutahiriwa. 27 Yahwe akamwambia Aroni, “Nenda nyikani ukutane
na Musa.” Aroni akaenda na kukutana naye katika mlima wa Mungu, na kumbusu.
28 Musa akwambia Aroni maneno yote ya Yahwe ambayo alimtuma kusema na kwa
habari za ishara zote za nguvu za Yahwe ambazo alimwagiza kutenda. 29 Kisha Musa
na Aroni wakaenda na kuwakusanya wazee wote wa Israeli. 30 Aroni akawaambia
maneno yote ambayo Yahwe alimwambia Musa. Pia alionesha ishara na miujiza ya
nguvu za Yahwe mbele ya watu. 31 Watu waliamini. Waliposikia ya kuwa Yahwe
aliwaona Waisraeli na ya kwamba aliyaona mateso yao, waliinamisha vichwa vyao
na kumwabudu.

# 5

1 Baada ya mambo haya kutokea, Musa na Aruni walienda kwa Farao na
kumwambia, ““Hivi ndivyo Yahwe, Mungu wa Israeli anasema: 'Waache watu wangu
waende, ili wapate kunifanyia karamu jangwani.'” 2 Farao akasema, “Yahwe ni
nani? Kwa nini mimi nisikiliz sauti yake na kuwaacha Israeli waende? Mimi
simjui Yahwe; na la zaidi, sitawaacha Israeli waende.” 3 Wakasema, “Mungu wa
Waebrania amekutana nasi. Tuache twende safari jangwani kwa siku tatu ili tutoe
sadaka kwa Yahwe Mungu wetu ili asituadhibu kwa mapigo au kwa upanga.”
4 Lakini mfalme wa Misri aliwaambia, “Musa na Aruni, kwa nini mnawatoa watu
kazini mwao? Nendeni kazini kwenu.” 5 Pia alisema, “Sasa kuna Waebrania
wengi nchini mwetu, na ninyi mnawafanya waache kazi zao.” 6 Siku ile ile, Farao
alitoa amri kwa wasimamizi na wanyapara wa wale watu. Akasema, 7 “Tofauti na
ilivyokuwa mwanzo, “Tofauti ni ilivyokuwa awali, msiwapatie tena watu majani ya
kutengenezea tofali. Waacheni wao waende kujitafutia majani wenyewe. 8 Ingawa
wanapaswa kuleta hesabu sawa ya matofali watakayotengeneza kama ilivyokuwa
awali. Msipokee pungufu, kwasababu wao ni wavivu. Ndiyo maana wanapiga kelele

na kusema, 'turuhusu tuende tukamtolee sadaka Mungu wetu.' 9 Waongezeeni kazi
wanaume ili wasipate tena muda wa kusikiliza maneno ya upotoshaji.” 10 Kwa hiyo
viongozi wa watu na waangalizi wao waliwajulisha watu. Walisema, “Hivi ndivyo
farao amesema: 'Sitawapeni tena malighafi. 11 Nyinyi wenyewe mtaenda kutafuta
majani popote mtakapopata, lakini kazi zenu hazitapunguzwa. 12 Basi watu hao
wakatawanyika katika nchi yote ya Misri ili wapate kukusanya matakataka badala
ya majani. 13 Wasimamizi wao wakawahimiza na kusema, “Malizeni kazi zenu,
sawa na wakati ule majani yalipokuwapo.” 14 Wanyapara wa Farao wakawapiga
wasimamizi wa Waisraeli, watu walewale ambao waliwaweka kuwa wasimamizi wa
watumishi. Wale Wanyapara wakakazana kuwauliza, “Kwanini hamjatimiza idadi
ya matofali inayotakiwa kwenu, siku ya jana na hata leo kama ambavyo mlifanya
siku za nyuma?” 15 Basi Wanyapara wa wana wa Israeli wakamwendea Farao na
kumlilia. Walisema, “Kwanini unawatendea watumishi wako hivi? 16 Sisi watumishi
wako hatupewi majani tena, lakini bado wanatuambia sisi, “Tengenezeni tofali!'
Sisi watumwa wako tunapigwa sasa, lakini kosa hilo ni la watu wako.” 17 Lakini
Farao akasema, “Ninyi ni wavivu! Wavivu ninyi! Ninyi mwasema, 'Turuhusu
twende kumtolea Yahwe sadaka.' 18 Sasa rudini kazini. Hamtapewa majani tena,
lakini mnapaswa kutengeneza idadi ile ile ya matofali.” 19 Wanyapara wa wana wa
Israeli wakagundua ya kuwa walikuwa kwenye shida kubwa mara walipoambiwa,
“Hamtapunguza kamwe idadi ya matofali mnayotengeneza kila siku.” 20 Wakakutana
na Musa na Haruni, waliokuwa wamesimama nje ya Ikulu wakati wanatoka kwa
Farao. 21 Wakawaambia Musa na Haruni, “Yahwe awatazame ninyi na kuwaadhibu,
kwa sababu mmetufanya sisi kuonekana wabaya mbele ya Farao na watumishi
wake. Mmetia upanga mikononi mwao ili watuue.” 22 Musa akarudi kwa BWANA
na kumwambia, “Bwana, kwanini umewatenda mabaya watu hawa? Kwanini
kunituma mimi kwanza? 23 Tangu nilipokuja kwa Farao kusema naye kwa jina lako,
amewatenda mabaya watu hawa, wala hujawaokoa watu wako hata kidogo.”

# 6

1 Kisha Yahweh akasema na Musa, “Sasa utaona nitakacho fanya kwa Farao. Utaona
hili, kwa kuwa ata waacha waenda kwa mkono wangu hodari. Kwasababu ya
mkono wangu hodari, ata waondoa nje ya nchi.” 2 Mungu akasema na Musa na
kumwambia, “Mimi ni Yahweh. 3 Nilimtokea Ibrahimu, Isaka, na Yakobo kama
Mungu mwenye nguvu; lakini kwa jina langu, Yahweh, sikujuliikana kwao. 4 Pia
niliimarisha agano langu na wao, ilikuwapatia nchi ya Kanani, nchi walioishi kama
sio raia, nchi walio tanga tanga. 5 Zaidi ya yote, nimesikia kilio cha Waisraeli ambao
wa Misri wame wa chukua watumwa, na nimekumbuka agano langu. 6 Kisha basi,
sema kwa Waisraeli, 'Mimi ni Yahweh. Nitawatoa kwenye utumwa chini ya wa Misri,
na kuwaweka huru na nguvu zao. Nitawaokoa kwa kudhihirisha nguvu zangu, na
kwa matendo ya ajabu ya hukumu. 7 Nitawaleta kwangu kama watu wangu, na
nitakuwa Mungu wenu. Mtajua kuwa mimi ndiye Yahweh Mungu wenu, aliye watoa
kwenye utumwa chini ya wa Misri. 8 Nitawaleta kwenye nchi niliyo muahidi kumpa
Ibrahimu, Isaka, na Yakobo. Nitawapa kama mali yenu. Mimi ni Yahweh.”' 9 Musa
alipo waambia haya Waisraeli, hawakumsiliza kwasababu ya mateso magumu ya
utumwa wao. 10 Hivyo Yahweh akazungumza na Musa na kumwambia, 11 “Nenda
umwambie Farao, mfalme wa Misri, awaache watu wa Israeli waondoke kwenye
nchi yake.” 12 Musa akamwambia Yahweh, “Kama Waisraeli hawajanisikiliza mimi,
kwa nini Farao anisikillize mimi, tangu mimi sio mzuri wakuzungumza?” 13 Yahweh
akasema na Musa na Aruni. Akawapa amri ya Waisraeli na Farao, mfalme wa Misri,
awatoe Waisraeli kutoka nchi ya Misri. 14 Hawa walikuwa vichwa wa nyumba za

baba yao: wana wa Rubeni, mzaliwa wa kwanza wa Israeli, walikuwa Hanoki, Palu,
Hezroni, na Karmi. Hawa walikuwa mababu wa ukoo wa Rubeni. 15 Wana wa
Simeoni walikuwa Yemueli, Yamini, Ohadi, Yakini, Zohari, na Shauli - mwana wa
mwanamke wa Kanani. Hawa walikuwa mababu wa ukoo wa Simeoni. 16 Hapa
yameorodheshwa majina ya wana wa Lawi, pamoja na uzo wao. Walikuwa ni
Gerishoni, Kohathi, na Merari. Lawi aliishi mpaka alipo kuwa na miaka 137. 17 Wana
wa Gerishoni walikuwa Libni na Shimei. 18 Wana wa Kohathi walikuwa Amramu,
Izhari, Hebroni, na uzieli. Kohathi aliishi hadi miaka 133. 19 Wana wa Merari
walikuwa Mahli na Mushi. Hawa walikuja kuwa mababu wa ukoo wa Walawi,
pamoja na uzao wao. 20 Amramu alimuoa Yokebedi, dada yake baba yake. Alimzalia
Aruni na Musa. Amramu aliishi miaka 137 na akafa. 21 Wana wa Izhari walikuwa
Kora, Nefegi, na Zikri. 22 Wana wa Uzieli walikuwa Mishaeli, Elizafani na Sithri.
23 Aruni alimuoa Elisheba, binti wa Aminadabu, dada wa Nashoni. Alimzaa Nadabu
na Abihu, Eleazari na Ithamari. 24 Wana wa Kora walikuwa Asiri, Elikana na Abiasa.
Hawa walikuwa mababu wa ukoo wa Wakora. 25 Eleazari, mwana wa Aruni, alimuoa
mmoja wa mabinti Wa Putieli. Alimzalia Fineazi. Hawa walikuwa vichwa wa nyumba
za baba yao miongoni mwa Walawi, pamoja na uzao wao. 26 Hawa wanaume wawili
walikuwa Musa na Aruni ambao Yahweh alisema, “Waleteni Waisraeli kutoka nchi
ya Misri, kwa makundi ya wanaume wapiganaji.” 27 Aruni na Musa wakazungumza
na Farao, mfalme wa Misri, awaruhusu Waisraeli watoke Misri. Hawa walikuwa
Musa na Aruni wale wale. 28 Pale Yahweh alipo zungumza na Musa katika nchi ya
Misri, 29 alimwambia, “Mimi ni Yahweh. Sema kwa Farao, mfalme wa MIsri, kila
kitu nitacho kwambia.” 30 Lakini Musa alimwambia Yahweh, “Mimi sio mzuri wa
kuongea, hivyo kwanini Farao anisikilize mimi?”

# 7

1 Yahweh akasema na Musa, “Ona, nimekufanya kama mungu kwa Farao. Aruni
kaka yako atakuwa nabii wako. 2 Utasema kila kitu nitacho kuamuru kusema.
Aruni kaka yako ata sema na Farao iliawaachie watu wa Israeli watoke kwenye
nchi yake. 3 Lakini nitaufanya moyo wa Farao mgumu, na nitaonyesha ishara
nyingi za nguvu zangu, maajabu mengi, katika nchi ya Misri. 4 Lakini Farao hata
kusikiliza, kwahiyo nitaueka mkono wangu juu ya Misri na kutoa makundi yangu
ya wanaume wapiganaji, watu wangu, wazao wa Israeli, watoke nchi ya Misri kwa
matendo makubwa ya hukumu. 5 Wamisri watajua kuwa mimi ni Yahweh nitapo
nyoosha mkono wangu kwa Misri na kuwatoa Waisraeli kutoka miongoni mwao.”
6 Musa na Aruni wakafanya hivyo; walifanya kama Yahweh alivyo waamuru. 7 Musa
alikuwa na miaka themanini, na Aruni miaka themanini na tatu walipo ongea na
Farao. 8 Yahweh akamwambia Musa na Aruni, 9 “Wakati Farao atakapo waambia,
'Fanya muujiza,' utamwambia Aruni, 'Chukuwa gongo lako na ulirushe chini mbele
ya Farao, ililigeuke nyoka.”' 10 Kisha Musa na Aruni wakaenda kwa Farao, na
wakafanya kama Yahweh alivyo waamuru. Aruni akarusha chini gongo lake mbele
ya Farao na watumishi wake, na likageuka nyoka. 11 Kisha naye Farao akawaita
wazee wenye hekima na wachawi. Wakafanya jambo hilo hilo kwa uchawi wao.
12 Kila mtu akarusha chini gongo lake, na magongo yakawa nyoka. Lakini gongo la
Aruni lilimeza nyoka zao. 13 Moyo wa Farao ulikuwa mgumu, na akusikiliza, kama
Yahweh alivyo tabiri. 14 Yahweh akasema na Musa, “Moyo wa Farao ni mgumu,
na anakataa kuacha watu waende. 15 Nenda kwa Farao asubui anapoenda kwenye
maji. Simama kwenye chanzo cha mto kukutana naye, na uchukuwe mkononi
mwako gongo ambalo liligeuka nyoka. 16 Mwambie, 'Yahweh, Mungu wa Waebrania,
amenituma kwako, “Acha watu wangu waende, iliwaniabudu nyikani. Mpaka sasa
haujanisikiliza.” 17 Yahweh anasema hili: “Kwa hili utajua kuwa mimi ni Yahweh.

Ninaenda kupiga maji ya mto wa Misri kwa gongo langu lililo mikono mwangu, na
mto utageuzwa kuwa damu. 18 Samaki walio kwenye mto watakufa, na mto utanuka.
Wa Misri Hawataweza kunywa maji yalio kwenye mto.”'" 19 Kisha Yahweh akasema
na Musa, “Mwambie Aruni, 'Chukuwa gongo lako na unyooshe mkono kwenye maji
ya Misri, na juu ya mito yake, mifereji, visima, na madimbwi yote, ili maji yao ya
damu. Fanya hivi ilikuwe na damu nchi nzima ya Misri, hadi kwenye vyombo vyote
vya mbao na mawe.”' 20 Musa na Aruni walifanya kama Yahweh alivyo waamuru.
Aruni alinyanyua gongo na kupiga maji ya mto, machoni pa Farao na watumishi
wake. Maji yote kwenye mto yaligeuga damu. 21 Samaki kwenye mto wakafa, na
mto ukaanza kunuka. Wamisri hawakuweza kunywa maji kwenye mto, na damu
ilikuwa kila mahali katika nchii ya Misri. 22 Lakini wachawi walifanya vivyo hivyo
na uchawi wao. Kwaiyo moyo wa Farao ukawa mgumu, na akakataa kuwasikiliza
Musa na Aruni, kama Yahweh alivyo sema itatokea. 23 Kisha Farao akarudi na kwenda
nyumbani kwake. Wala hakutilia maanani hili. 24 Wamisri wote walichimba pembeni
ya mto kwa ajili ya maji ya kunywa, lakini hawakuweza kunywa maji ya mto. 25 Siku
saba zilipita baada ya Yahweh kushambulia mto.

# 8

1 Kisha Yahweh akazungumza na Musa, “Nenda kwa Farao na umwambie, 'Yahweh
anasema hivi: Acha watu wangu waende hili wakaniabudu. 2 Ukikataa kuwaruhusu
waende, nitaidhuru nchi yako yote kwa vyura. 3 Mito itajawa na vyura. Watatoka
na kuingia nyumbani kwako, chumbani kwako, na kitandani kwako. Wataenda
nyumbani mwa watumishi wako. Wataenda kwa watu wako, kwenye majiko yako,
na vyombo vya kukandia mkate. 4 Vyura watakushambulia wewe, watu wako, na
watumishi wako wote."”' 5 Yahweh akamwambia Musa, “Mwambie Aruni, 'Nyoosha
mkono wako na gongo lako kwenye mito, mifereji, na kwenye mabwawa, na uwatoe
vyura juu ya nchi ya Misri.”' 6 Aruni akanyoosha mkono juu ya maji ya Misri, na
vyura wakatoka na kujaza nchi ya Misri. 7 Lakini wachawi walifanya vivyo hivyo
na uchawi wao: waliwatoa vyura juu ya nchi ya Misri. 8 Kisha Farao akawaita
Musa na Aruni na kuwaambia, “Muombeni Yahweh iliawaondoe vyura kwangu na
kwa watu wangu. Kisha nitawaacha watu waende, iliwamtolee dhabihu.” 9 Musa
akamwambia Farao, “Unaweza chukuwa fursa ya kuniambia lini nikuombee wewe,
watumishi wako, na watu wako, ili vyura waondolewe kwako na nyumbani kwako
na wabaki tu kwenye mito.” 10 Farao akasema, “Kesho.” Musa akasema, “Acha iwe
kama ulivyo sema, ili kwamba ujue hakuna Mungu mwengine kama Yahweh, Mungu
wetu. 11 Vyura wataondoka kutoka kwako, nyumbani mwako, kwa watumishi wako,
na kwa watu wako. Watabaki tu kwenye mito.” 12 Musa na Aruni wakaondoka
kwa Farao. Kisha Musa akamlilia Yahweh kuhusu hao vyura alio waleta kwa
Farao. 13 Yahweh akafanya kama Musa alivyo omba: Vyura wakafa kwenye nyumba,
nyuani, na mashambani. 14 Watu wakawakusanya kwa mafungu, na nchi ikanuka.
15 Lakini Farao alipoona kuna afadhali, aliufanya moyo wake kuwa mgumu na
hakumsikiliza Musa na Aruni, kama Yahweh alivyo sema. 16 Yahweh akamwambia
Musa, “Mwambie Aruni, 'Nyoosha gongo lako na upige udongo chini, iliuwe chawa
kati nchi yote ya Misri.”' 17 Wakanya hivyo: Aruni akanyoosha mkono wake na
gongo lake. Akaupiga udongo wa ardhi. Chawa wakaja juu ya watu na wanyama.
Udongo wote kwenye ardhi ukawa chawa katika nchi ya Misri. 18 Wachawi walijaribu
kufanya chawa kwa uganga wao lakini hawakuweza. Palikuwa na chawa kwa
watu na kwa wanyama. 19 Kisha wachawi wakamwambia Farao, “Hichi ni kidole
cha Mungu.” Lakini moyo wa Farao ulikuwa Mgumu, hivyo akakataa kuwasikiliza.
Ilikuwa kama Yahweh alivyo sema Farao atafanya. 20 Yahweh akamwambia Musa,

“Inuka asubui mapema na usimame mbele ya Farao anapoenda mtoni. Umwambie,
'Yahweh anasema hivi: “Acha watu wangu waende wakaniabudu mimi. 21 Lakini
usipo acha watu wangu waende nitatuma kundi la nzi kwako, watumishi wako, na
watu wako, na kwenye nyumba zenu. Nyumba za wa Misri zitajawa na makundi
ya nzi, na ata ardhi wanayo simama itajawa na nzi. 22 Lakini katika siku hiyo
nitaitendea nchi ya Gosheni tofauti, nchi ambayo watu wangu wanaishi, ilikwamba
kusiwe na makundi ya nzi huko. Hili litatokea ili kwamba mjue mimi ni Yahweh
katika hii nchi. 23 Nitaweka utofauti kati ya watu wangu na watu wako. Hii ishara
ya nguvu zangu itatokea kesho"”' 24 Yahweh akafanya hivyo, na kundi kubwa la nzi
likaja nyumbani mwa Farao na nyumbani mwa watumishi wake. Katika nchi yote
ya Misri, nchi iliharibiwa na makundi ya nzi. 25 Farao akawaita Musa na Aruni na
kuwaambia, “Nendeni, mtolee Mungu wenu dhabihu kwenye nchi yetu.” 26 Musa
akasema, “Sio vyema sisi kufanya hivyo, kwa kuwa dhabihu tunazo mtolea Yahweh
Mungu wetu zinachukiza kwa Wamisri. Kama tutatoa dhabihu mbele ya macho
yao zilizo chukizo kwa Wamisri, hawata tupiga mawe? 27 Hapana, ni safari ya siku
tatu kwenda nyikani ambayo lazima tuende, ili kiutoa dhabihu kwa Yahweh Mungu
wetu, kama anavyo tuamuru.” 28 Farao akasema, “Nitakuruhusu kwenda kumtolea
dhabihu Yahweh Mungu wenu nyikani. Ila usiende mbali sana. Niombee.” 29 Musa
akasema, “Wakati tu nitakapoenda kutoka kwako, nitamuomba Yahweh ili makundi
ya nzi yatoke kwako, wewe Farao, na watumishi wako na watu kesho. Lakini usifanye
udhalimu tena kwa kutowaacha watu wetu waende kumtolea dhabihu Yahweh.”
30 Musa akaenda nje kutoka kwa Farao na kumuomba Yahweh. 31 Yahweh akafanya
kama Musa alivyo muomba: alitoa makundi ya nzi kutoka kwa Farao, watumishi
wake, na watu wake. Hakuna ata mmoja aliye baki. 32 Lakini Farao aliufanya moyo
wake mgumu tena, na hakuwaacha watu waende.

# 9

1 Kisha Yahweh akamwambia Musa, Nenda kwa Farao na umwambie, 'Yahweh,
Mungu wa Waebrania, anasema hivi: “Acha watu wangu waende ili wakaniabudu
mimi.” 2 Lakini ukikataa kuwaruhusu waende, kama utaendelea kuwa bakiza nyuma,
3 basi mkono wa Yahweh utakuwa kinyume dhidi ya mifugo yako shambani na kwa
farasi, punda, ngamia, ng'ombe na kondoo, naitasababisha ugonjwa mbaya sana.
4 Yahweh ata tendea tofauti mifugo ya Israeli na mifugo Misri: Haukuna mnyama
wa Waisraeli ataye kufa. 5 Yahweh ametenga muda; amesema, “Ni kesho ambapo
nitafanya ilitukio katika nchi."”' 6 Yahweh akafanya hivi siku iliyofuata: mifugo yote
ya Misri ikafa. Lakini hamna mnyama wa Waisraeli aliye kufa, hamna mnyama ata
mmoja. 7 Farao akafanya utafiti, na tazama, hakuna mnyama ata mmoja aliye kufa.
Lakini moyo wake ulikuwa mjeuri, hivyo hakuwaacha watu waende. 8 Kisha Yahweh
akawambia Musa na Aruni, “Chukuwa majivu na uyajaze mkononi kutoka kwenye
tanuru. Wewe, Musa, lazima uyarushe juu wakati Farao akitazama. 9 Yatakuwa
vumbi safi nchi nzima ya Misri. Yatasababisha majipu na mafua kulipuka kwa watu
na wanyama katika nchi yote ya Msri.” 10 Hivyo Musa na Aruni wakachukuwa
majivu kutoka kwenye tanuru na kusimama mbele ya Farao. KIsha Musa akarusha
majivu juu. Majivu yakasababisha majipu na mafua kutokea kwa watu na wanyama.
11 Waganga hawakuweza kumzuia Musa kwasababu ya majipu, kwasababu majipu
yalikuwa kwao na kwa Wamisri wote. 12 Yahweh akaufanya moyo wa Farao kuwa
mgumu, Farao hakuwasikiliza Musa na Aruni. Hili ndilo Yahweh alilo mwambia
Musa Farao atalo fanya. 13 Kisha Yahweh akamwambia Musa, Amka asubui mapema,
simama mbele ya Farao, na umwambie, 'Yahweh, Mungu wa Waebrania, anasema
hivi: Acha watu wangu waende ili wakaniabudu mimi. 14 Kwa muda huu nitatuma

mapigo kwako wewe, kwa watumishi wako na watu wako. Nitafanya hivi ili ujue
hakuna kama mimi kwenye dunia yote. 15 Mpaka sasa ningeweza kuunyosha mkono
wangu na kukushambulia wewe na watu wako kwa ugonjwa, na ungeondelewa
kwenye nchi. 16 Lakini ni kwa sababu hii nimekuruhusu uishi: ili kukuonyesha
nguvu zangu, ili kwamba jina langu litangazwe dunia nzima. 17 Bado unajiinua
dhidi ya watu wangu kwa kuwaacha wasiende. 18 Sikiliza! Kesho muda kama huu
nita leta mvua ya mawe ya barafu kubwa, kama ambayo haijawai kuonekana Misri
toka ilipo anza hadi sasa. 19 Kisha sasa, tuma wanaume na ukusanye mifugo yako
na vitu vyote ulivyo navyo mashambani sehemu salama. Kila mtu na mnyama
aliyeko shambani na hajaletwa nyumbani - mawe ya barufu yatawashukia, na
watakufa."”' 20 Kisha hao wa watumishi wa Farao walio amini ujumbe wa Yahweh
waka harakisha kuleta watumwa na mifugo yao ndani ya nyumba zao. 21 Lakini
hao ambao hawa kuchukuwa ujumbe wa Yahweh maanani waliacha watumwa wao
na mifugo shambani. 22 Kisha Yahweh akamwambia Musa, “Nyoosha mkono wako
kuelekea mbingu ili kuwe na mawe ya barafu katika nchi yote ya Misri, kwa watu,
kwa wanyama, na kwenye mimea yote shambani na nchi nzima ya Misri.” 23 Musa
akanyoosha mkono na gongo lake kuelekea mbiguni, na Yahweh akatuma mngurumo,
mawe ya barafu, na radi kwenye nchi. Pia alinyesha mvua kwenye nchi ya Misri.
24 Hivyo kulikuwa na radi iliyo changanyika na mawe ya barafu, ilikuwa hatari sana,
kuliko yeyote iliyowai kutokea kwenye nchi ya Misri tangu liwe taifa. 25 Katika nchi
yote ya Misri, barafu ya mawe ilipiga kila kitu kwenye shamba, watu na wanyama.
Ilipiga kila mmea shambani na kuvunja kila mti. 26 Isipo kuwa tu nchi ya Gosheni,
walipo ishi Waisraeli, hapakuwa na mawe ya barafu. 27 Kisha Farao akatuma
wanaume wakawaite Musa na Aruni. Akawaambia, “Nimetenda dhambi wakati huu.
Yahweh ni mwenye haki, na mimi na watu wangu ni waovu. 28 Muombe Yahweh,
kwasababu radi na barafu ya mawe imezidi. Nitawaacha muende, na hamtabaki
tena hapa.” 29 Musa akamwambia, “Nitakapo ondoka tu kwenye mji, nitaitanua
mikono yangu kwa Yahweh. Mngurumo utaacha, na hakutakuwa na barafu ya mawe
tena. Kwa ili utajua kuwa nchi ni ya Yahweh. 30 Lakini kwa wewe na watu wako,
najua bado hamu mheshimu Yahweh Mungu.” 31 Sasa kitani na shayiri ziliharibiwa,
kwa kuwa shayiri ilikuwa katika kukomaa, na kitani ilikuwa imestawi. 32 Lakini
ngano na kusemethu hazikupigwa mana zinachelewa kukua. 33 Musa alipo muacha
Farao na mji, alitanua mikono yake kwa Yahweh; mngurumo na barafu ya mawe
ikasimama, na mvua haikunyesha tena. 34 Farao alipoona mvua, barafu ya mawe,
na mngurumo umekatika, akatenda dhambi na kufanya moyo wake kuwa mgumu,
pamoja na watumishi wake. 35 Moyo wa Farao ulikuwa mgumu, hakuacha watu wa
Israeli waende. Hivi ndivyo Yahweh alimwambia Musa Farao atafanya.

# 10

1 Yahweh akamwambia Musa, “Nenda kwa Farao, kwa kuwa nimeufanya moyo
wake mgumu na moyo wa watumishi wake. Nimefanya hivi kuonyesha hizi ishara
za nguvu zangu miongoni mwao. 2 Pia nimefanya hivi ili muwaambie watoto wenu
na wajukuu wenu vitu nilivyo fanya, jinsi nilivyo itendea Misri kwa ukali, na jinsi
nilivyo onyesha aina tofauti za ishara za nguvu zangu miongoni mwao. Kwa hili
mtajua kuwa mimi ni Yahweh.” 3 Hivyo Musa na Aruni wakaenda kwa Farao
na kumwambia, “Yahweh, Mungu wa Waebrania, anasema hivi: 'Kwa muda gani
utaendelea kukataa kujinyenyekesha mbele zangu? Acha watu wangu waenda ili
wakaniabudu. 4 Lakini ukikataa kuwaruhusu watu wangu kwenda, sikiliza, kesho
nitaleta nzige kwenye nchi yako. 5 Watafunika ardhi ya juu ili kwamba mtu asiweze
kuona udongo. Watakula mabaki yote yalio salia kwenye mvua ya barafu ya

mawe. Pia watakula kila mti unaokua shambani. 6 Watajaza nyumba zenu, zote za
watumishi wenu, na zote za Wamisri wote - jambo ambalo baba zenu wala mababu
zenu hawakuwai kuona, jambo ambalo halikuwai shuhudiwa toka walipo kuwa
duniani hadi leo."' Kisha Musa akaondoka na kutoka kwa Farao. 7 Watumishi wa
Farao wakamwambia, "Mpaka lini huyu mwanaume ata kuwa msumbufu kwetu?
Acha Waisraeli waende wakamuabudu Yahweh Mungu wao. Bado haujatambua
kuwa Misri imeharibiwa?" 8 Musa na Aruni wakaletwa tena kwa Farao, ambaye
aliwaambia, "Nendeni amkamuabudu Yahweh Mungu wenu. Lakini watu gani
wataenda?" 9 Musa akasema, "Tutaondoka na wadogo wetu na wakubwa wetu,
pamoja na wana wetu na mabinti zetu. Tutaondoka na ng'ombe na kondoo zetu,
maana lazima tufanye siku kuu ya Yahweh." 10 Farao akawaambia, "Yahweh kwa
kweli awe nanyi, kama nitawaacha muende na wadogo zenu waende. Angalia, una
uovu kwenye nia. 11 Hapana! Nenda, wanaume tu miongoni mwenu, na mmuabudu
Yahweh, kwa kuwa hilo ndilo mnalo litaka." Kisha Musa na Aruni wakaondolewa
uweponi mwa Farao. 12 Kisha Yahweh akamwambia Musa, "Nyoosha mkono wako
kwenye nchi ya Misri palipo na nzige, ili washambulie nchi ya Misri na kula kila
mmea, kila kitu barua ya mawe iliyo acha." 13 Musa akanyoosha na gongo lake
juu ya nchi ya Misri, na Yahweh akaleta upepo wa mashariki juu ya nchi mchana
wote na usiku mzima. Palipo kuwa asubui, upepo wa mashariki ulileta nzige.
14 Nzige wakaenda nchi yote ya Misri na kuharibu sehemu zote. Hapajawai kuwa na
kundi kama hilo la nzige juu ya nchi, hakuna kama tena kama hilo litawai kutokea.
15 Walifunika ardhi yote ya juu ikawa giza. Walikula kila mmea na kila tunda la miti
ambayo barafu ya mawe ilibakiza. Kila eneo la nchi ya Misri, hakuna mmea wa kijani
ulibaki, wala mti au mmea wa shambani. 16 Kisha Farao akawaita Musa na Aruni
na kuwaambia, "Nimefanya dhambi dhidi ya Yahweh na dhidi yako. 17 Kisha sasa,
nisamehe dhambi yangu wakati huu, na uombe kwa Yahweh Mungu wako aondoe
hichi kifo kwangu." 18 Musa akaondoka kwa Farao na kumuomba Yahweh. 19 Yahweh
akaleta upepo mkali wa magharibi ulio wachukuwa wale nzige na kuwapeleka Bahari
ya Shamu; hakuna nzige ata mmoja aliye baki eneo la Misri. 20 Lakini Yahweh
aliufanya moyo wa Farao mgumu, na Farao hakuacha Waisraeli waende. 21 Kisha
Yahweh akamwambia Musa, "Nyoosha mkono wako kuelekea mbingu, ili kuwe na
giza nchi yote ya Misri, giza linalo weza kuhisiwa." 22 Musa akanyoosha mkono
wake kuelekea mbingu, na kulikuwa na giza nene nchi yote ya Misri kwa siku tatu.
23 Hakuna aliye muona mwingine; hakuna aliye toka nyumbani mwake kwa siku
tatu. Walakini, Waisraeli wote walikuwa na taa katika sehemu walizo ishi. 24 Farao
alimuita Musa na kusema, "Nenda umuabudu Yahweh. Ata familia zenu za weza
kwenda nanyie, lakini ng'ombe zenu na kondoo zenu zitabaki." 25 Lakini Musa
akasema, "Lazima utupe wanyama kwa ajili ya dhabihu na sadaka za kuteketeza ili
tuwatoe dhabihu kwa Yahweh Mungu wetu. 26 Mifugo yetu lazima iende na sisi; ata
mmoja hawezi kubaki, lazima tuwapeleke wakamuabudu Yahweh Mungu wetu. Kwa
kuwa hatujui tutakacho muabudu nacho Yahweh mpaka tufike pale. 27 Lakini Yahweh
aliufanya moyo wa Farao mgumu, na hakuwaacha waende. 28 Farao alimwambia
Musa, "Toka kwangu! Kuwa muangalifu na jambo moja, kwamba usinione tena, kwa
kuwa siku utakapo uona uso wangu, utakufa." 29 Musa akasema, "Wewe mwenyewe
umesema. Sitauona uso wako tena."

# 11

1 Kisha Yahweh akamwambia Musa, "Bado kuna pigo moja nitalo lileta kwa
Farao na Misri. Baada ya hilo, atakuacha uondoke hapa. Atakapo kuachia uende,
ata kuondoa kabisa. 2 Waelekeze watu kwamba kila mwanaume na mwanamke
amuulizie jirani yake vitu vya fedha na vitu vya dhahabu." 3 Sasa Yahweh

aliwafanya Wamisri kuwa na shauku ya kuwapendeza Waisraeli. Aidha, Musa
alikuwa wakuvutia sana machoni pa watumishi wa Farao na watu wa Misri. 4 Musa
akasema, “Yahweh asema hivi: 'Wakati wa usiku wa manane nitaenda Misri yote.
5 Wazaliwa wa kwanza wote wa nchi ya Misri watakufa, kuanzia mzaliwa wa
kwanza wa Farao, anaye keti kiti chake cha enzi, mpaka mzaliwa wa kwanza wa
misichana mtumwa anaye saga mbegu, na kwa wazaliwa wa kwanza wa mifugo.
6 Kisha kutakuwa na kilio kikubwa nchi yote ya Misri, kama ambacho hakijawai wala
hakitatokea tena. 7 Lakini ata mbwa hata bweka kwa watu wa Israeli, dhidi ya mtu
au mnyama. Kwa hili utajuwa kuwa nina watendea Wamisri na Waisraeli tofauti.'
8 Watumishi wote hawa wako, Farao, watakuja chini yangu na kunisujudu mimi.
Watasema, 'Nenda, wewe na watu wote wanao kufuata!' Baada ya hapo nitaondoka.”
Kisha akaondoka mbele ya Farao kwa hasira kubwa. 9 Yahweh akamwambia Musa,
Farao hatakusikiliza. Hii ni ili nifanye mambo ya ajabu katika nchi ya Misri.” 10 Musa
na Aruni wakafanya mambo haya ya kushangaza mbele za Farao. Lakini Yahweh
aliufanya moyo wa Farao mgumu, na Farao hakuwaacha watu wa Israeli kuondoka
katika nchi yake.

# 12

1 Yahweh akasema na Musa na Aruni katika nchi ya Misri. Alisema, 2 “Kwako
wewe, mwezi huu utakuwa mwanzo wa miezi, mwezi wa kwanza wa mwaka
kwako. 3 Liambie kusanyiko la Israeli, 'Siku ya kumi mwezi huu kila mtu lazima
achukuwe mwana kondoo au mbuzi mdogo wa kwake, kila familia ifanye hivi,
mwana kondoo kwa kila nyumba. 4 Kama hiyo nyumba ni ndogo sana kwa mwana
kondoo, mwanaume na jirani yake wachukuwe mwana kondoo au nyama ya mbuzi
mdogo ambayo itatosha watu. Lazima iwe yatosha kwa kila mtu kula, kwaiyo lazima
wachukuwe nyama ya kutosha kulisha wote. 5 Mwana kondoo wako au mbuzi
wako mdogo lazima asiwe na upungufu, dume mwenye mwaka mmoja. Unaweza
kuchukuwa mmoja wa kondoo au mbuzi. 6 Lazima umtunze mpaka siku ya kumi na
nne ya huo mwezi. Kisha kusanyiko lote la Israeli lazima liwaue hawa wanyama jioni.
7 Lazima uchukuwe baadhi ya damu na uweke kwenye sehemu mbili za mihimili ya
milango na juu ya fremu za milango ambapo utalia hizo nyama. 8 Lazima ule hizo
nyama usiku, baada ya kuchoma kwenye moto. Kula na mkate ulio andaliwa kwa
hamira, pamoja na mimea michungu. 9 Usiile mbichi au imechemshwa kwenye maji.
Badala yake, choma kwenye moto na kichwa chake, miguu na sehemu za ndani.
10 Usiache ata kidogo kubaki mpaka asubui. Lazima uchome chochote kilicho baki
asubui. 11 Hivi ndivyo wa paswa kula: ukiwa umefunga mkanda wako, umevaa viatu
vyako, na gongo lako mkononi mwako. Lazima ule kwa haraka. Ni Pasaka ya Yahweh.
12 Yahweh anasema hili: Nitaenda katika nchi ya Misri usiku na kushambulia
wazaliwa wote wa kwanza wa wanadamu na wanyama katika nchi ya Misri. Nitaleta
pigo kwa miungu yote ya Misri. Mimi ni Yahweh. 13 Damu itakuwa ishara kwenye
nyumba zenu ya kuja kwangu. Nitakapo ona damu, nitapita nitakapo shambulia
nchi ya Misri. Ili pigo halitawajia na kuwaharibu. 14 Hii siku itakuwa kumbukumbu
kwenu, ambayo lazima muadhimishe kama sherehe ya Yahweh. Itakuwa sheria
kwenu pia, kwenye vizazi vyote vya watu wenu, ambayo mwapaswa kuadhimisha
leo. 15 Utakula mkate bila hamira wakati wa siku saba. Siku ya kwanza utaondoa
hamira kwenye nyumba zenu. Yeyote atakaye kula mkate uliyotiwa chachu kwanzia
siku ya kwanza mpaka siku ya saba, huyo mtu lazima akatwe kutoka Israeli. 16 Siku
ya kwanza kutakuwa na kusanyiko lililo tengwa kwa ajili yangu, na siku ya saba
kutakuwa na kusanyiko kama hilo. Hakuna kazi itakayo fanywa hizi siku, zaidi ya
kupika kila mmoja ale. Hiyo ndio kazi pekee itakayo fanywa na wewe. 17 Lazima

uadhimishe hii Sherehe ya Mkate Usiotiwa Chachu kwasababu ni siku hii ambayo
nitawaleta watu wako, makundi yaliyo na silaha, kwa makundi yaliyo na silaha,
kutoka nchi ya Misri. Lazima uadhimishe hii siku kwa vizazi vyote vya watu wako.
Hii itakuwa sheria kwako. 18 Lazima ule mkate usiotiwa chachu kuanzia jioni ya siku
ya kumi na nne ya mwezi wa kwanza wa mwaka, mpaka jioni ya siku ya ishirini na
moja ya mwezi. 19 Wakati wa hizi siku, nyumbani mwenu kusipatikane na hamira.
Yeyote atakaye kula mkate ulio andaliwa na hamira lazima akatwe kutoka jamii ya
Israeli, huyo mtu awe ni mgeni au mtu aliye zaliwa nchini mwenu. 20 Hautakula
chochote kilicho andaliwa na hamira. Popote utapo ishi, lazima ule mkate usio na
hamira."' 21 Kisha Musa akawaita viongozi wote wa Israeli na kuwaambia, "Nendeni
na mchague mwana kondoo au mbuzi watakao tosha kulisha familia zenu na muue
mwana kondoo wa pasaka. 22 Kisha chukua jani la hisopu na uchovye kwenye damu
itakayo kuwa kwenye beseni. Paka damu iliyo kwenye beseni juu ya fremu ya
mlango na kwenye mihimili miwili ya mlango. Hakuna ata mmoja atakaye toka
nje ya mlango wake mpaka asubui. 23 Kwa kuwa Yahweh atapita kushambulia
Wamisri. Atakapo ona damu juu ya fremu ya mlango na kwenye mihimili miwili
ya mlango, atapita mlango wako na ata ruhusu mharibifu kuja nyumbani kwenu
kuwashambulia. 24 Lazima uadhimishe hili tukio. Hili litakuwa daima sheria kwako
na kwa uzao wenu. 25 Utakapo ingia nchi Yahweh atakayo kupa, kama alivyo
ahidi kufanya, lazima uadhimishe hili tendo la ibada. 26 Watoto wako watakapo
kuuliza, 'Hili tendo la ibada lina maana gani?' 27 kisha lazima useme, 'Ni sadaka
ya Pasaka ya Yahweh, kwasababu Yahweh kapita nyumba za Waisraeli Misri alipo
washambulia Wamisri. Aliweka nyumba zetu huru."' Kisha watu wakamsujudia
Yahweh. 28 Waisraeli wakaenda na kufanya kama Yahweh alivyo waamuru Musa na
Aruni. 29 Ikawa usiku wa manane kuwa Yahweh akawashambulia wazaliwa wote wa
kwanza wa nchi ya Misri, kuanzia mzaliwa wa kwanza wa Farao, aliye keti kiti chake
cha enzi, mzaliwa wa kwanza wa mtu aliye gerezani na wazaliwa wote wa kwanza
wa mifugo. 30 Farao akaamka usiku - yeye, watumishi wake, na Wamisri. Palikuwa na
kelele za maombolezo Misri, kwa kuwa hakukuwa na nyumba ambayo hamna mtu
hakufa. 31 Farao akamuita Musa na Aruni usiku na kusema, "Inuka, tokeni miongoni
mwa watu wangu, nyie pamoja na Waisraeli. Nenda, mmuabudu Yahweh, kama
mlivyo sema mnataka kufanya. 32 Chukuweni ng'ombe zenu na kondoo zenu, kama
mlivyo sema, na muende, na pia mnibariki." 33 Wamisri walikuwa na haraka ya kuwa
ondoa nchini, kwa kuwa walisema, "Sisi ni watu tuliokufa." 34 Watu wakachukuwa
ngano yao pasipo kuongeza hamira yeyote. Bakuli zao zakukandia ngano zilifungiwa
kwenye nguo zao na kwenye mabega yao. 35 Watu Waisraeli walifanya kama Musa
alivyo waambia. Waliwaomba Wamisri vitu vya fedha, vitu vya dhahabu, na nguo.
36 Yahweh aliwafanya Wamisri na shauku ya kuwapendeza Waisraeli. Hivyo Wamisri
waliwapa chochote walicho waomba. Katika hili, Waisraeli waliwachukulia vingi
Wamisri. 37 Waisraeli wakasafiri kutoka Ramesi kwenda Sakothi. Walikuwa na
idadi ya wanaume 600, 000 kwa miguu, kuongezea kwa wanawake na watoto.
38 Mchanganyiko wa kundi la wasio Waisraeli pia walienda nao, pamoja na ng'ombe
na kondoo, idadi kumbwa ya mifugo. 39 Walioka mikate na unga wa ngano wenye
hamira walio utoa Misri. Ulikuwa hauna hamira kwasababu waliondolewa Misri
na hawakuweza chelewa kuandaa chakula. 40 Waisraeli waliishi Misri kwa miaka
430. 41 Baada ya miaka 430, siku hiyo hiyo, majeshi yote ya Yahweh yalio jiami
waliondoka kutoka nchi ya Misri. 42 Huu ulikuwa usiku wakuwa macho, ili Yahweh
awatoe kutoka nchi ya Misri. Huu ulikuwa usiku wa Yahweh wa kuadhimishwa
na Waisraeli wote na watu wa vizazi vyao vyote. 43 Yahweh akamwambia Musa na
Aruni, "Hii ni sheria ya Pasaka: hakuna mgeni anaye ruhusiwa kuila. 44 Walakini, kila
mtumwa wa Misraeli, aliye nunuliwa kwa pesa, anaeza kula baada ya kutahiriwa.

45 Wageni na watumishi waajiriwa hawapaswi kula chakula chochote. 46 Chakula
chapaswa kuliwa ndani ya nyumba moja. Hauruhusiwi kubeba nyama yeyote nje ya
nyumba, na hauruhusiwi kuvunja mfumba wowote. 47 Jamii zote za Israeli za paswa
kuadhimisha sherehe. 48 Kama mgeni anaishi na wewe na anataka kuadhimisha
Pasaka kwa Yahweh, ndugu zake wote wa kiume wapaswa kutahiriwa. Kisha anaeza
kuja na kuadhimisha. Atakuwa kama watu walio zaliwa kwenye nchi. Walakini,
hakuna mtu asiye tahiriwa anaruhusiwa kula chakula chochote. 49 Sheria hii hii
itahusika kwa mzaliwa wa asili na mgeni anayeishi miongoni mwenu." 50 Waisraeli
wote walifanya kama Yahweh alivyo waamuru Musa na Aruni. 51 Ikaja kuwa siku
hiyo Yahweh akawaleta Israeli kutoka nchi ya Misri kwa makundi yalio jiami.

# 13

1 Yahweh akasema na Musa na kumwambia, 2 "Nitengee wazaliwa wote wa kwanza,
kila mzaliwa wa kwanza wa Waisraeli, watu na wanyama. Mzaliwa wa kwanza ni
wangu." 3 Musa akawambia watu, "Hii kumbukeni hii siku, siku mliyo toka Misri,
kutoka nyumba ya utumwa, kwa mkono hodari wa Yahweh amewatoa kutoka hii
sehemu. Hakuna mkate wa hamira waruhusiwa kuliwa. 4 Mnatoka Misri hii siku,
mwezi wa Abibu. 5 Yahweh atakapo waleta nchi ya Wakanani, Wahiti, Waamori,
Wahivi, na Wayebusi, nchi aliyo waapia mababu zenu kuwapa, nchi inayo tiririka
kwa maziwa na asali - kisha wapaswa kuadhimisha hili tendo la ibada kila mwezi.
6 Kwa siku saba utakula mkate bila hamira; siku ya saba kutakuwa na maakuli ya
kumuadhimisha Yahweh. 7 Mkate usio na hamira wapaswa kuliwa kwa siku saba
zote; hakuna mkate ulio na hamira wapaswa kuliwa miongoni mwenu. Hakuna
hamira yapaswa kuonekana kwenye mipaka yenu. 8 Hiyo siku utasema kwa watoto
wako, 'Hii ni kwasababu ya kile Yahweh alichofanya kwangu nilipo taka Misri.' 9 Hii
itakuwa kumbukumbu mkononi mwako, na kumbukumbu kwenye paji la uso wako.
Hii ni ili sheria ya Yahweh iwe kinywani mwako, maana kwa mkono hodari Yahweh
amewatoa kutoka Misri. 10 Kisha basi wapaswa kushika hii sheria kwa wakati uliyo
kusudiwa kutoka mwaka hadi mwaka. 11 Yahweh atakapo waleta kwenye nchi ya
Wakanani, kama alivyo apa kwenu na kwa mababu zenu kufanya, na atakapo wapa
nchi ninyi, 12 lazima umtengee mzaliwa wa kwanza mtoto na uzao wa kwanza wa
wanyama wenu. Wakiume watakuwa wa Yahweh. 13 Kila mzaliwa wa kwanza
wa punda lazima umnunue tena na mwana kondoo. Kama hautamnunua tena,
lazima uivunje shingo yake. Lakini kila mzaliwa wa kwanza wakiume miongoni
mwenu - lazima umnunue tena. 14 Mwanae atakapo kuuliza baadae, 'Hii ina maana
gani?' kisha utamwambia, 'Ni kwa mkono hodari Yahweh katutoa Misri, kutoka
nyumba ya utumwa. 15 Farao alipo kataa kwa ujeuri kutuachia twende, Yahweh
aliwaua wazaliwa wa kwanza wa nchi ya Misri, wazaliwa wa kwanza wa watu na wa
wanyama. Ndio sababu ninatoa dhabihu kwa Yahweh kwa kila mzaliwa wa kwanza
wa kila mnyama, na pia sababu nina nunua wazaliwa wa kwanza wa wanangu
tena.' 16 Hii itakuwa kumbukumbu mikononi mwako na kumbukumbu kwenye
paji lako la uso, kwa kuwa ni kwa mkono hodari Yahweh alitutoa kutoka Misri."
17 Farao alipo waachia watu waende, Mungu akuwaongoza kwa njia ya Wafilisti,
japo hiyo njia ilikuwa karibu. Kwa kuwa Mungu alisema, "Labda watu watabadili
nia zao watakapo ona vita na watarudi Misri." 18 Hivyo Mungu akawaongoza
watu kuzunguka nyikani kupita Bahari ya Shamu. Waisraeli waliondoka kutoka
nchi ya Misri wakiwa wamejiami kwa pambano. 19 Musa akachukuwa mifupa ya
Yusufu pamoja naye, kwa kuwa Yusufu aliwaapisha Waisraeli na kusema, "Mungu
atawaokoa, na muibebe mifupa yangu na nyie." 20 Waisraeli walisafiri kutoka Sakothi
na kuweka kambi Ethamu pembezoni mwa nyikani. 21 Yahweh alitangulia mbele

yao mchana kama nguzo ya wingu kuwaongoza njiani. Usiku alienda kama nguzo
ya moto kuwapa mwanga. Kwa namna hii waliweza kusafiri mchana na usiku.
22 Yahweh hakuchukuwa kutoka kwa watu nguzo ya wingu mchana wala nguzo ya
moto usiku.

# 14

1 Yahweh akasema na Musa na kumwambia, 2 “Waambie Waisraeli wageuke na
kueka kambi mbele ya Pi Hahirothi, katikati ya Migdoli na bahari, mbele ya Baali
Zefoni. Wapaswa kueka kambi pembenni ya Pi Hahirothi. 3 Farao atasema kuhusu
Waisraeli, 'Wanaangaika kwenye nchi. Nyikani imewafunika.' 4 Nitaufanya moyo wa
Farao mgumu, na yeye ata wakimbiza. Nitapata utukufu kwasababu ya Farao na
jeshi lake lote. Wamisri watajua mimi ni Yahweh.” Kisha Waisraeli wakaeka kambi
kama walivyo elekezwa. 5 Mfalme wa Misri alipo ambiwa Waisraeli wametoroka,
nia ya Farao na watumishi wake ikageuka dhidi ya watu. Wakasema, “Tumefanya
nini kwa kuwaacha Waisraeli waende huru na wasitutumikie?” 6 Kisha Farao
akachukuwa magari yake ya farasi na jeshi lake. 7 Alichukuwa magari ya farasi
mia sita imara na magari yote ya farasi ya Misri, pamoja na maafisa wa hayo
magari. 8 Yahweh akafanya mgumu moyo wa Farao, mfalme wa Misri, na mfalme
akawafukuzia Waisraeli. Sasa Waisraeli waliondoka kwa shangwe. 9 Lakini Wamisri
wali wafukuzia, pamoja na farasi na magari ya farasi, wapanda farasi, na jeshi lake.
Walikuta Waisraeli wameeka kambi pembezoni mwa bahari kati ya Pi Hahirothi na
Baali Zefoni. 10 Farao alipo karibia, Waisraeli walitaza juu na kushangaa. Wamisri
walikuwa wakija kwao, na waliogopa. Waisraeli walimlilia Yahweh. 11 Walimwambia
Musa, “Ni kwasababu hakukuwa na makaburi Misri, hadi umetuleta tufe huku
nyikani? Kwanini umetutendea hivi, kwa kututoa Misri? 12 Hili si ndilo tulilo
kwambia Misri? Tulikwambia, 'Utuache, ili tuwafanyie Wamisri kazi.' Ingekuwa
bora kwetu sisi kuwafanyia kazi kuliko kufa nyikani.” 13 Musa akawaambia watu,
“Msiogope. Simameni imara na muone wokovu Yahweh atakao uleta kwenu leo. Kwa
maana hamtawaona tena Wamisri mnao waona leo. 14 Yahweh ata wapigania, na
ninyi mtasima imara.” 15 Kisha Yahweh akamwambia Musa, “Kwanini wewe, Musa,
unaendelea kuniita mimi? Waambie Waisraeli waendelee mbele. 16 Nyanyua gongo
lako juu, nyoosha mkono wako kuelekea baharini na uigawanye sehemu mbili, ili
watu wa Israeli wapite baharini kwenye nchi kavu. 17 Jitahadharishe kuwa nitafanya
mioyo ya Wamisri kuwa migumu ili wawafuate. Nitapata utukufu kwasababu ya
Farao na jeshi lake lote, magari yake ya farasi, na wapanda farasi. 18 Kisha Wamisri
watajua kuwa mimi ni Yahweh nitakapo pata utukufu kwasababu ya Farao, magari
yake ya farasi, na wapanda farasi wake.” 19 Malaika wa Mungu, aliyeenda mbele
ya Waisraeli, aliama na kwenda nyuma yao. Nguzo ya wingu ili sogea mbele yao
na kwenda kusimama nyumba yao. 20 Wingu lilikuja katikati ya kambi ya Misri
na kambi ya Israeli. Lilikuwa wingu jeusi kwa Wamisri, lakini liliangaza usiku
kwa ajili ya Waisraeli, hivyo upande mmoja haukuweza kuja karibu ya mwingine
usiku wote. 21 Musa akanyoosha mkono wake kuelekea bahari. Yahweh akasogeza
bahari nyuma kwa upepo mkali wa mashariki usiku huo wote na kufanya bahari
nchi kavu. Kwa namna hii maji yaligawanyika. 22 Waisraeli walienda katikati ya
bahari kwa nchi kavu. Maji yaliunda ukuta mkono wao wa kulia na mkono wao
wa kushoto. 23 Wamisri waka wafukuzia. Wali wafuata hadi katikati ya bahari
- farasi wote wa Farao, magari ya farasi, na wapanda farasi. 24 Lakini masaa ya
mapema ya asubui, Yahweh alitazama chini jeshi la Wamisri kupitia nguzo ya moto
na wingu. Alisababisha hofu miongoni mwa Wamisri. 25 Magari yao ya farasi
yalikuwa yana kwama matairi, na wapanda farasi waliendesha kwa ugumu. Hivyo

Wamisri walisema, “Acha tuwakimbie Waisraeli, kwa kuwa Yahweh anawapigania
dhidi yetu.” 26 Yahweh akamwambia Musa, “Nyoosha mkono kuelekea bahari ili maji
yawarudie Wamisri, magari yao ya farasi, na wapanda farasi wao.” 27 Hivyo Musa
akanyoosha mkono wake kuelekea bahari, na ikarudi kwenye hali yake ya kawaida
palipo pambazuka. Wamisri walikimbilia ndani ya bahari, na Yahweh akawaingiza
Wamisri katikati ndani yake. 28 Maji yakarudi na kufunika magari ya farasi ya Farao,
wapanda farasi, na jeshi lake lote lililo fuata magari ya farasi kwenye bahari. Hakuna
aliyepona. 29 Walakini, Waisraeli walitembea kwenye nchi kavu katikati ya bahari.
Maji yalikuwa ukuta kwao mkono wa kulia na mkono wa kushoto. 30 Hivyo Yahweh
akaokoa Israeli hiyo siku kutoka mkono wa Wamisri, na Israeli ikaona maiti za
Wamisri ufukweni. 31 Israeli ilipoona nguvu kubwa Yahweh aliyo itumia dhidi ya
Wamisri, watu walimsifu Yahweh, na kumwamini Yahweh na mtumishi wake Musa.

# 15

1 Kisha Musa na watu wa Israeli wakaimba hii nyimbo kwa Yahweh. Waliimba,
“Nitaimba kwa Yahweh, kwa kuwa ameshinda kwa utukufu; farasi na dereva
wake amewatupa kwenye bahari. 2 Yahweh ni uweza wangu na nyimbo yangu,
na amekuwa wokovu wangu. Huyu ni Mungu wangu, na nitamsifu, Mungu wa
baba yangu, nitamtukuza. 3 Yahweh ni shujaa; Yahweh ni jina lake. 4 Ametupa
magari ya farasi ya Farao na jeshi lake kwenye bahari. Maafisa wa Farao hodari
walizama kwenye Bahari ya Shamu. 5 Kina kiliwafunika; walienda kwenye kina
kama jiwe. 6 Mkono wako wakulia, Yahweh, una nguvu ya utukufu; mkono wako,
Yahweh, umewavunja adui. 7 Kwa utukufu mkubwa umewapindua walio inuka
dhidi yako. Umetuma gadhabu; imewateketeza kama karatasi. 8 Kwa pumzi ya
pua yako maji yalijaa; maji yanayo tembea yalisimama wima na kujaa juu; maji
yalikuwa manene ndani ya kilindi cha bahari. 9 Adui alisema, 'Nitakimbiza, nitapita,
nitagawa nitakacho chukuwa; tamanio langu litatimizwa kwao; nitavuta upanga
wangu; mkono wangu utawaharibu wao.' 10 Lakini ulipuliza kwa upepo wako, na
bahari ikawafunika wao; walizama kama chuma nzito kwenye maji mengi. 11 Ni
nani kama wewe, Yahweh, miongoni mwa miungu? Nani kama wewe, mtakatifu wa
utukufu, katika sifa umetukuzwa, anaye fanya miujiza? 12 Ulinyoosha mkono wako
wa kulia, na dunia ikawameza. 13 Katika uaminifu wa agano lako umewaongoza watu
ulio waokoa. Katika uweza wako umewaongoza katika sehemu takatifu unayo ishi.
14 Watu watasikia, na watatetemeka; hofu itawakumba wakazi wa Filistia. 15 Kisha
wazee wa Edomu wataogopa; wanajeshi wa Moabu watetemeka; wakazi wote wa
Kanani watayayuka. 16 Mshituko na hofu vitawaangukia. Kwasababu ya nguvu ya
mkono wako, watakuwa kimya kama jiwe hadi watu wako watakapo pita, Yahweh
- hadi watu ulio waokoa watakapo pita. 17 Utawaleta na kuwapanda kwenye mlima
wa urithi wako, sehemu, Yahweh, ulio jenga ya kuishi, sehemu takatifu, Bwana wetu,
mikono yako iliyo jenga. 18 Yahweh ata tawala milele na milele.” 19 Kwa kuwa
farasi wa Farao walienda na magari ya farasi na wapanda farasi kwenye bahari.
Yahweh alileta maji ya bahari juu yao. Lakini Waisraeli walienda juu ya nchi kavu
katikati ya bahari. 20 Miriamu nabii wa kike, dada wa Aruni, akanyanyua tari,
na wanawake wote wakatoka na matari, wakicheza nae. 21 Miriamu akawaimbia:
“Muimbieni Yahweh, kwa kuwa ameshinda kwa utukufu. Farasi na mpanda farasi
amewatupa baharini. 22 Kisha Musa akaongoza Israeli mbele kupita Bahari ya Shamu.
Walienda nyikani ya Shuri. Walisafiri kwa siku tatu nyikani pasipo kuona maji
yeyote. 23 Kisha wakaja Mara, lakini hawakunywa maji ya huko kwasababu yalikuwa
machungu. Hivyo wakaita hiyo sehemu Mara. 24 Hivyo watu wakamlalamikia Musa
na kusema, “Nini tunaweza kunywa?” 25 Musa akamlilia Yahweh, na kumonyesha

mti. Musa akautupa kwenye maji, na maji yakawa matamu kunywa. Ndio pale
Yahweh alipowapa sheria kali, na ndio pale alipo wajaribu. 26 Alisema, “Kama
utasikiliza sauti ya Yahweh Mungu wako kwa umakini, na kufanya yalio sahihi
machoni pake, na kama utatega sikio kwa amri zake na kutii sheria zake zote -
sitawaekea ninyi magonjwa yale niliyo waekea Wamisri, kwa kuwa mimi ni Yahweh
ninaye kuponya.” 27 Kisha watu wakaja Elimu, palipo kuwa na chemichemi kumi na
mbili za maji na miti sabini ya mtende. Walieka kambi hapo pembeni ya maji.

# 16

1 Watu wakaendelea na safari kutoka Elimu, na jamii yote ya Waisraeli ikaja nyikani
mwa Sinu, iliyopo katikati ya Elimu na Sinai, siku ya kumi na tano ya mwezi wa
pili walipo toka Misri. 2 Jamii yote ya Waisraeli wali walalamikia Musa na Aruni
nyikani. 3 Waisraeli waliwaambia, “Kama tu tungekufa kwa mkono wa Yahweh nchi
ya Misri tulipo kuwa tumeketi kwenye vyombo vya nyama na tulikuwa tunakula
mkate kwa tele. Maana umetuleta nyikani uuwe jamii zetu zote kwa njaa.” 4 Kisha
Yahweh akamwambia Musa, “Nitakunyeshea mvua ya mkate. Watu wataenda na
kukusanya kiasi cha siku kila siku ili niwajaribu kama wataendelea kushika sheria
yangu au hapana. 5 Itakuja kuwa siku ya sita, kwamba watakusanya mara mbili
zaidi ya wanavyo kusanyaga, na watapika wanacholeta.” 6 Kisha Musa na Aruni
wakawaambia watu wote wa Israeli, “Jioni mtajua kuwa ni Yahweh aliye waleta
kutoka nchi ya Misri. 7 Asubui utaona utukufu wa Yahweh, kwa maana anasikia mna
mlalamikia. Sisi ni nani hadi mtulalamikie?” 8 Musa pia akasema, “Utajua hili pale
Yahweh atakapo kupa nyama jioni na mkate asubui kwa tele - kwa kuwa amesikia
malalamishi mnayo tamka dhidi yake. Nani ni Aruni na mimi? Malalamishi yenu
sio dhidi yetu; ni dhidi ya Yahweh.” 9 Musa akamwambia Aruni, “Sema kwa jamii
yote ya watu wa Israeli, 'Njoo karibu ya Yahweh, kwa kuwa amesikia malalamishi
yenu.'” 10 Ikawa, Aruni alipo sema na jamii yote ya watu wa Israeli, wakaangalia
kuelekea nyikani, na, tazama, utukufu wa Yahweh ukatokea kwenye wingu. 11 Kisha
Yahweh akasema na Musa na kumwambia, 12 “Nimesikia malalamishi ya watu wa
Israeli. Sema nao na useme, 'Jioni utakula nyama, na asubui utashiba mkate. Kisha
utajua mimi ni Yahweh Mungu wako.'” 13 Ikaja kuwa kwamba jioni kware wakaja juu
na kufunika kambi. Asubui umande ulitanda kambini. 14 Umande ulipo kwisha, pale
juu ya ardhi ya nyikani kulikuwa na kama barafu iliyo ganda kwenye ardhi. 15 Watu
wa Israeli walipo ona, walisema mmoja kwa mwenzake, “Hii ni nini?” Hawakujua
ilikuwa ni nini. Musa akawaambia, “Ni mkate Yahweh aliyo wapa mle. 16 Hii ni amri
Yahweh aliyotoa: 'Lazima ukusanye, kila mmoja wenu, kiasi unacho itaji kula, lita
mbili kwa kila mtu. Hivi ndivyo utakavyo kusanya: Kusanya cha kutosha kula cha
kila mtu anaye ishi hemani mwako.'” 17 Watu wa Israeli wakafanya hivyo. Baadhi
wakakusanya zaidi, baadhi wakakusanya kidogo. 18 Walipo pima kwa kipimo cha lita,
hao walio kusanya zaidi hawakuwa na kilicho salia, na hao walio kusanya kidogo
hawakuwa na pungufu. Kila mmoja alikusanya cha kutosha kukidhi maitaji yake.
19 Kisha Musa akawaambia, “Hakuna ata mmoja kubakiza hadi asubui.” 20 Walakini,
hawakumsikiliza Musa. Baadhi yao waliacha baadhi hadi asubui, lakini ilizalisha
wadudu na kuwa batili. Kisha Musa akawa na hasira juu yao. 21 Walikusanya
asubui kwa asubui. Kila mtu alikusanya cha kutosha kula kwa hiyo siku. Jua
lilipo kuwa kali, ili yayuka. 22 siku ya sita walikusanya mkate mara mbili zaidi,
lita mbili kwa kila mtu. Viongozi wote wa jamii walikuja na kumwambia hili kwa
Musa. 23 Aliwaambia, “Hili ndilo Yahweh alililo lisema: 'Kesho ni mapumziko ya
kujiliwaza, sabato takatifu kwa utukufu wa Yahweh. Oka kile unataka kuoka, na
chemsha kile unataka kuchemsha. Vyote vitakavyo baki, jihifadhie hadi asubui.”'

24 Hivyo wakaeka pembeni hadi asubui, kama Musa alivyo elekeza. Haikuharibika,
wala haikuwa na mdudu yeyote. 25 Musa alisema, “Kula hicho cha kula leo, kwa
kuwa leo ni siku iliyo tengwa ya kumtukuza Yahweh. Leo hamtaikuta mashambani.
26 Mtaikusanya ndani ya siku sita, lakini siku ya saba ni Sabato. Siku ya Sabato hakuta
kuwa na manna.” 27 Ilikuja kuwa siku ya saba ambapo baadhi ya watu walienda
kukusanya manna, lakini hawakukuta 28 Kisha Yahweh akamwambia Musa, Kwa
muda gani utaendelea kukataa kushika amri zangu na sheria zangu? 29 Tazama,
Yahweh amekupa Sabato. Hivyo siku ya sita anakupa mkate wa siku mbili. Kila
mmoja wenu lazima akae kwenye sehemu yake; hakuna hata mmoja wa kutoka
sehemu yake siku ya saba.” 30 Hivyo watu watapumzika siku ya saba. 31 Watu wa
Israeli walikiita chakula kile “manna.” Ilikuwa ni nyeupe kama mbegu ya mgiligani,
na ladha yake kama maandazi yaliyo pikwa na asali. 32 Musa akasema, “Hili ndilo
Yahweh alilo amuru: 'Acha lita mbili ya manna ihifadhiwe kwa ajili vizazi vya watu
wako ili kwamba uzao wako uone mkate niliyo kulisha nyikani, baada ya kukutoa
kutoka nchi ya Misri. 33 Musa akamwambia Aruni, “Chukuwa jagi na uweke lita mbili
za manna ndani yake. Hifadhi kwa Yahweh i dumu vizazi vyote vya watu.” 34 Kama
Yahweh alivyo muamuru Musa, Aruni akahifadhi pembeni mwa mawe yaliyo kuwa
na amri za agano. 35 Watu wa Israeli walikula manna miaka arobaini mpaka walipo
kuja nchi yenye watu. Walikula mpaka walipo fika kwenye mipaka ya nchi ya Kanani.
36 Lita mbili ni makumi ya efa.

# 17

1 Jamii yote ya Israeli ili safiri kutoka nyikani ya Sinu, wakifuata maelekezo ya
Yahweh. Walieka kambi Refidimu, lakini hapakuwa na maji ya watu kunywa. 2 Hivyo
watu wakamlaumu Musa kwa hali yao na kusema, “Tupe maji ya kunywa.” Musa
akasema, “Kwanini mnagombana na mimi? Kwanini mnajaribu Yahweh?” 3 Watu
walikuwa na kiu sana, na waka mlalamikia Musa. Wakasema, “Kwanini umetutoa
Misri? Ili utuue sisi na watoto wetu na mifugo yetu kwa kiu?” 4 Kisha Musa akamlilia
Yahweh, “Nini ni fanya kwa hawa watu? Wako tayari ata kunipiga mawe.” 5 Yahweh
akamwambia Musa, “Nenda mbele yao, na uchukuwe baadhi ya wazee wa Israeli.
Chukuwa gongo ulilo piga nalo mto, na uende. 6 Nitasimama mbele yako pale
kwenye mwamba wa Horebu, na utaupiga mwamba. Maji yatatoka ya watu kunywa.”
Kisha Musa akafanya hivyo mbele ya wazee wa Israeli. 7 Aliita ile sehemu Massa
na Meriba kwasababu ya malalamishi ya Waisraeli, na kwasababu walimjaribu
Bwana kwa kusema, “Je Yahweh yupo miongoni mwetu au hapana?” 8 Kisha jeshi
la watu wa Ameleki wakaja na kushambulia Israeli huko Refidimu. 9 Hivyo Musa
akamwambia Yoshua, “Chagau wanaume kadha na uende nje. Pigana na Ameleki.
Kesho nitasimama juu ya kilima na gongo la Mungu mkononi mwangu.” 10 Hivyo
Yoshua akapigana na Ameleki kama Musa alivyo elekeza, wakati Musa, Aruni, na
Huri walienda juu ya kilima. 11 Wakati Musa alipo kuwa ameshikilia mikono yake
juu, Israeli ilikuwa yashinda; alipo acha mikono yake ipumzike, Ameleki alianza
kushinda. 12 Mikono ya Musa alipo kuwa mizito, Aruni na Huri walichukuwa jiwe na
kuweka chini yake alikalie. Muda huo huo, Aruni na Huri walinyanyua mikono yake
juu, mtu mmoja upande mmoja, na mtu mmoja upande mwingine. Hivyo mikono ya
Musa ilishikiliwa tuli mpaka jua lilipo zama. 13 Hivyo Yoshua akawashinda watu wa
Ameleki kwa upanga. 14 Yahweh akamwambia Musa, “Andika haya kwenye kitabu na
umsomee Yoshua, kwasababu nitaondoa kumbukumbu ya Ameleki kutoka chini ya
mbingu.” 15 Kisha Musa akajenga madhabahu na kuiita “Yahweh ni bendera yangu.”
16 Alisema, “Kwa kuwa mkono ulinyanyuliwa juu kuelekea kiti cha enzi cha Yahweh
- kwamba Yahweh ata fanya vita na Ameleki vizazi na vizazi.”

# 18

1 Yethro, kuhani wa Midiani, baba mkwe wake Musa, alisikia yote Mungu aliyo
fanya kwa Musa na kwa Israeli watu wake. Alisikia Yahweh ametoa Israeli kutoka
Misri. 2 Yethro, baba mkwe wake Musa, akamchukuwa Zipora, mke wa Musa,
baada ya kumpeleka nyumbani, 3 na wana wake wawili; jina mmoja lilikuwa
Gershomu, kwa kuwa Musa alisema, “Nimekuwa mgeni katika nchi ya kigeni.” 4 Jina
la mwingine lilikuwa Eliezeri, kwa kuwa Musa alisema, “Mungu wa babu yangu
alikuwa msaada wangu. Aliniokoa na mkono wa Farao.” 5 Yethro, baba mkwe
wake Musa, alikuja na watoto wake Musa na mke wake Musa nyikani alipo eka
kambi katika mlima wa Mungu. 6 Alimwambia Musa, “Mimi, baba mkwe wako
Yethro, nina kuja kwako na mke wako na wanao wawili.” 7 Musa alitoka kwenda
kukutana na baba mkwe wake, akamwinamia, na kumbusu. Wakajuliana hali na
wakaingia ndani ya hema. 8 Musa akamwambia baba mkwe wake yale yote Yahweh
aliyo ya fanya kwa Farao na Wamisri kwa ajili ya Waisraeli, magumu yote yaliyo
watoke njianim na jinsi Yahweh alivyo waokoa. 9 Yethro akafurahia yale mema
yote Yahweh aliyo watendea Israeli, kwa hilo amewaokoa na mkono wa Wamisri.
10 Yethro akasema, “Yahweh atukuzwe, kwa kuwa amekuokoa na mkono wa Wamisri
na mkono wa Faraom na kuwatoa watu kwenye mkono wa Wamisri. 11 Sasa najua
Yahweh ni mkuu kuliko miungu yote, kwasababu Wamisri walipo watenda Waisraeli
kwa kiburi, Mungu aliwaokoa watu wake.” 12 Yethro, baba mkwe wake Musa, akaleta
sadaka ya kuteketeza na dhabihu kwa Mungu. Aruni na wazee wote wa Israeli
wakaja kula chakula mbele za Yahweh na baba mkwe wake Musa. 13 Siku iliyofuata
Musa aliketi kuwa hukumu watu. Watu walisimama kumzunguka Musa kwanzia
asubui hadi jioni. 14 Baba mkwe wake Musa alipo ona yale yote aliyo yafanya kwa
watu, alisema, “Ni nini unachofanya na watu? Kwanini unaketi peke yako na watu
wote wamesimama kukuzunguka asubui hadi jioni?” 15 Musa akamwambia baba
mkwe wake, “Watu wanakuja kuniuliza muongozo wa Mungu. 16 Wanapo kuwa
na malumbano, wanakuja kwangu. Ninaamua kati ya mtu mmoja na mwingine,
na nina wafundisha maagizo na sheria.” 17 Baba mkwe wake Musa alimwambia,
“Unachofanya sicho kizuri sana. 18 Hakika utajichosha, wewe na watu waliyopo na
wewe. Huu mzigo ni mzito sana kwako. Hauwezi kufanya peke yako. 19 Nisikilize.
Nitakupa ushauri, na Mungu ata kuwa na wewe, kwasababu wewe nimwakilishi
wa watu kwa Mungu, na una leta malumbano yao kwake. 20 Lazima uwafundishe
maagizo yake na sheria. Lazima uwafundishe njia yakutembea na kazi ya kufanya.
21 Mbali zaidi, lazima uchague wanaume wenye uwezo kutoka watu wote, wanaume
wanao muheshimu Mungu, wanaume wa kweli wanao chukuia mapato ya ufisadi.
Lazima uwaeke juu ya watu, kuwa viongozi wa maelfu, mamia, hamsini, na makumi.
22 Watawa hukumu watu na kesi za kawaida, lakini kesi ngumu wataleta kwako. Kwa
kesi ndogo, wanaweza kuhukumu wenyewe. Kwa hivyo itakuwa rahisi kwako, na
watabeba mzigo na wewe. 23 Ukifanya hivi, na kama Mungu akikuamuru kufanya al
kadhalika, basi utaweza kuvumilia, na watu wote watarudi nyumbani wameridhika.”
24 Hivyo Musa akasikiliza maneno ya baba mkwe wake na akafanya yale yote aliyo
yasema. 25 Musa alichagua wanaume wenye uwezo kutoka Israeli na kuwa fanya
vichwa juu ya watu, viongozi wahusika wa maelfu, mamia, hamsini, na makumi.
26 Waliwa hukumu watu katika hali za kawaida. Kesi ngumu walimletea Musa, lakini
wao wenyewe wali hukumu kesi ndogo. 27 Kisha Musa akamwacha baba mkwe wake
kuondoka, na Yethro akarudi kwenye nchi yake.

# 19

1 Katika mwezi wa tatu baada ya watu wa Israeli kutoka Misri, siku hiyo,

walikwenda nyikani ya Sinai. 2 Walipo ondoka Refidimu na kuja nyikani ya Sinai,
walieka kambi mbele ya mlima. 3 Musa akaenda juu kwa Mungu. Yahweh alimuita
kutoka mlimani na kusema, “Lazima uiambie nyumba ya Yakobo, watu wa Israeli:
4 Uliona nilicho fanya kwa Wamisri, jinsi nilivyo kubeba kwa mabawa ya tai na
kukuleta kwangu. 5 Kisha sasa, ukinisikiliza kwa utii sauti yangu na kushika agano
langu, kisha utakuwa mali yangu ya pekee miongoni mwa watu wote, kwa kuwa
dunia yote ni yangu. 6 Utakuwa ufalme wa kikuhani na taifa takatifu langu. Haya
ni maneno wapaswa kuwaambia Waisraeli. 7 Hivyo Musa akaja na kuwaita wazee
wa watu. Aliweke mbele yao maneno yote haya Yahweh aliyo muamuru. 8 Watu
wote walijibu pamoja na kusema, “Tutafanya yote Yahweh aliyo tuambia.” Kisha
musa akaja kutoa taarifa ya maneno watu kwa Yahweh. 9 Yahweh akamwambia
Musa, “Nitakuja kwako kwa wingu nene ili watu wasikie ninapo sema na wewe na
wakuamini milele.” Kisha Musa kamwambia Yahweh maneno ya Yahweh. 10 Yahweh
akamwambia Musa, “Nenda kwa watu. Leo na kesho lazima uwatenge, na kuwafanya
waoshe mavazi yao. 11 Kuwa tayari kwa siku ya tatu, kwa kuwa siku ya tatu Yahweh
atashuka chini ya Mlima Sayuni. 12 Lazima uweke mipaka kote kuzunguka mlima
kwa ajili ya watu. Uwaambie, 'Kuweni waangalifu msiende juu ya mlima au kushika
mipaka yake. Yeyote atakaye shika mlima ata uawa.' 13 Hakuna mkono wa mtu yeyote
kumshika mtu huyu. Badala yake, lazima apigwe mawe au kuchomwa mshale. Iwe ni
mtu au mnyama, lazima auawe. Tarumbeta itakapo pigwa muda mrefu, wanaweza
kuja chini ya mguu wa mlima.” 14 Kisha Musa akashuka mlimani kwenda kwa watu.
Aliwatenga watu kwa ajili ya Yahweh na wakaosha mavazi yao. 15 Aliwaambia watu,
“Kuweni tayari siku ya tatu; msiwakaribie wake zenu.” 16 Siku ya tatu, ilipo fika
asubui, kulikuwa na ngurumo na radi na wingu nene kwenye mlima, na sauti kubwa
ya tarumbeta. Watu wote kambini waliogopa. 17 Musa akaleta watu kutoka kambini
kukutana na Mungu, na wakasimama miguuni mwa mlima. 18 Mlima Sina ulijwa
kabisa na moshi kwasababu Yahweh alishuka na moto na moshi. Moshi ulipanda juu
kama moshi wa tanuru, na mlima wote ulitikisika kwa vurugu. 19 Sauti ya tarumbeta
ilipo ongezeka na zaidi, Musa akazungumza, na Mungu kamjibu kwa sauti. 20 Yahweh
akashuka chini ya Mlima Sinai, juu ya mlima, na akamuita Musa kuja juu. Kisha Musa
akapanda juu. 21 Yahweh akamwabia Musa, “Shuka chini na uwaonye watu wasipite
kuniangalia, au wengi wao wataangamia. 22 Acha pia mukuhani wanao kuja karibu
yangu wakitenge - wajiandae kwa ujio - ili nisiwashambulie.” 23 Musa akamwabia
Yahweh, “Watu hawawezi kuja juu ya mlima, kwa kuwa umetuamuru: 'Eka mipaka
kuzunguka mlima na utenge kwa ajili ya Yahweh.'” 24 Yahweh akamwambia, Nenda,
shuka chini ya mlima, na umelete Aruni na wewe, lakini usiache makuhani na watu
kupita vizuizi na kuja kwangu, au nitawashambulia.” 25 Hivyo Musa akaenda chini
kwa watu na kusema nao.

# 20

1 Mungu alisema maneno yote haya: 2 Ndimi Bwana Mungu wenu, niliyewatoa
katika ardhi Misri, nje ya nyumba ya utumwa. 3 Msiwe na miungu mingine ila mimi
tu. 4 Msijitengenezee sanamu za kuchonga kufananisha na kitu chochote kilichopo
juu ya mbingu, chini ya ardhi, au ndani ya maji. 5 Msipinde na kuabudu sanamu,
mimi Yahweh Mungu wenu, ni Mungu mwenye wivu. Nitaadhibu uovu wa mababu
kwa kuleta adhabu juu ya kizazi, cha tatu hadi kizazi cha nne kwa wale wanao
nichukia. 6 Ila nitaweka agano la uaminifu kwa maelfu watakao nipenda na kushika
amri zangu. 7 Usilitaje bure jina la Yahweh Mungu wako, sitkuwa na hatia kwa yeyote
atakaye taja jina langu bure. 8 Ikumbuke siku ya Sabato, na kunitengea. 9 lazima
ufanye kazi zako zote kwa siku sita. 10 Ila siku ya saba ni Sabato kwaajili ya Yahweh

Mungu wako. Siku hiyo usifanye kazi yoyote, wewe, au mwana wako, au binti yako,
au mtumishi wako wakiume, au mtumishi wako mwanamke, au ng'ombe zako, au
mgeni aliye ndani ya malango yako. 11 Kwa siku sita Yahweh aliumba mbingu na
nchi, bahari, na vitu vyote vilivyomo, na siku ya saba alipumzika. Kwa hiyo Yahweh
aliibariki siku ya Sabato na kuitenga. 12 Waheshimu baba na mama yako, ili uweze
kuishi miaka mingi duniani Yahweh Mungu wako ametoa. 13 Usiue. 14 Usifanye
uasherati (usizini). 15 Usiibe kwa mtu yoyote. 16 Usishuhudie uongo dhidi ya jirani
yako. 17 Usitaman nyumba ya jirani yako; usitamani mke wa jirani yako, wala
mtumishi wake wakiume, mtumishi wake mwanamke, ng'ombe wake, punda wake,
au chochote cha jirani yako. 18 Watu wote waliona radi na umeme, na kusikia sauti
ya mbiu, na mlima ukitoa moshi. Watu walipoona hivo, walitetemeka na kusimama
mbali. 19 Wakamwambia Musa, ongea na sisi, na tutakusikiliza; lakini usiruhusu
Mungu kuongea nasi, ama tutakufa. 20 Musa akawaambia watu, “msiogope, Mungu
alikuja kuwajaribu ili heshima yake iwe ndani yenu, kwa hiyo msitende dhambi.”
21 hivyo watu walisimama mbali, na Musa alikaribia giza nene Mungu alipokuwa.
22 Yahweh alimwambia Musa, “Ni lazima uwaambie hili Waisraeli: 'Wewe mwenyewe
umeona niliongea na wewe kutoka mbinguni. 23 Misjitengenezee miungu mingine
pamoja nami, miungu ya fedha au miungu ya dhahabu. 24 Tengenezeni madhabahu
ya udongo kwa ajili yangu, na lazima mtoe sadaka ya kuteketeza, sadaka ya ushirika,
kondoo, na ng'ombe. kila sehemu ntakapotaka jina langu liheshimiwe, nitakuja
kwenu na kuwabariki. 25 Kama mtatengeneza madhabahu ya mawe, msijenge na
mawe yaiyokatika, na kama mtatumia vyombo vyenu juu yake, mtaweka unajisi.
26 msije juu ya madhabahu yangu kwa hatua zenu; hii ni ili msioneshe sehemu zenu
za siri.”

# 21

1 Sasa hizi ni amri utakazoweka kabla yao: 2 'kama mtanunua mtumishi wa
kiebrania, atatumikia kwa miaka sita, na mwaka wa saba ataachiwa huru bila
kilipwa chochote. 3 Kama alikuja mwenyewe, ataenda huru kwa ridhaa yake; 4 kama
bwana wake atampa mke na kumzalia mwana na binti, mke pamoja na watoto wake
watabaki mali ya bwana wake, na ataenda zake huru. 5 Lakini kama mtumishi
atasema waziwazi, “Nampenda bwana wangu, mke wangu, na watoto; sitaenda nje,”
6 “kisha bwana wake atapaswa kumleta kwa Mungu. Bwana wake atapaswa kumleta
katika mlango au katika muhimili wa mlango, na bwana wake atatoboa sikio lake
na sindano. Kisha mtumishi wake atamtumikia kwa maisha yake yote. 7 Kama
mwanaume ata muuza binti wake kama mtumishi wa kike, ata weza kwenda huru
kama watumishi wa kiume wanavyo enda. 8 Kama hamridhishi bwana wake, aliye
mtenga kwa ajili yake, kisha lazima amnunue tena. Hana ruhusa ya kumuuza kwa
watu wengine wa kigeni. Hana ruhusa hiyo, sababu amemtendea kwa hila. 9 Ikiwa
bwana wake atamposa awe mke wa mwanae, atamtendea kama desturi zipasavyo
sawa na binti zake. 10 Ikiwa atajitwalia mke mwingine, asimpunguzie huyo chakula
chake, nguo na haki zake za unyumba. 11 Lakini asipofanyiwa mambo haya matatu,
basi anaweza kwenda bure pasipo kutolewa mali. 12 Mtu awaye yote ampigaye mtu
hata akafa, inampasa mtu huyo auawe pia. 13 Lakini kama hakumvizia, ila kwa bahati
mbaya, basi nitamfanyia mahali pa kukimbilia. 14 Lakini mtu akimwendea mwenzake
kwa kujikinai, kusudi apate kumwua kwa hila; huyo utamwondoa hata kama ni
madhabahuni pangu, ili auawe. 15 Yeyote atakaye mpiga baba au mama yake lazima
auawe. 16 Yeyote atakaye mteka mtu na kumuuza, au mtu amekutwa kama mali yake,
huyo mtekaji lazima auawe. 17 Yeyote atakaye mlaani baba au mama yake lazima
auawe. 18 Kama wanaume watapigana na mmoja akimpiga mwengine kwa jiwe au

ngumi, na huyo mtu asife, lakini alazwe kitandani; 19 kisha akapona na anaweza
kutembea kwa gongo lake, yeye aliye mpiga lazima alipe muda aliye mpotezea; na
lazima alipe matibabu yake yote. Lakini huyo mtu hana hatia ya mauaji. 20 Kama
mwanaume akimpiga mtumishi wake wa kiume au wa kike kwa gongo, na kama
mtumishi huyo akifa kwa madhara ya pigo, kisha huyo mtu lazima ahadhibiwe.
21 Walakini, mtumishi huyo akiishi siku moja au mbili, bwana aruhusiwi kuadhibiwa,
kwa kuwa atateseka kupoteza mtumishi huyo. 22 Kama wanaume wakipigana pamoja
na wakamuumiza wanamke mwenye mimba na kuiharibu, lakini hakuna majeraha
mengine kwake, kisha huyo mwanaume mwenye hatia lazima alipe kama mme wa
mwanamke anavyo taka kwake, na kulipa kama hakimu anavyo kusudia. 23 Lakini
kama kuna majeraha makubwa, lazima utoe uhai kwa uhai, jicho kwa jicho, 24 jino
kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu, 25 kuchoma kwa kuchoma, jeraha
kwa jeraha, au mkwaruzo kwa mkwaruzo. 26 Kama mwanaume akipiga jicho la
mtumishi wake kiume au mtumishi wake wa kike na kuliharibu, kisha lazima
amuache mtumishi aende pasipo fidia ya jicho. 27 Kama akitoa jino la mtumishi wake
wa kiume au mtumishi wake wa kike, lazima amuache mtumishi kwenda huru kama
fidia ya jino. 28 Kama ng'ombe akimpiga mwanaume au mwanamke akafa, ng'ombe
lazima apigwe mawe, na nyama yake hairuhusiwi kuliwa; lakini mmiliki wa ng'ombe
lazima awe huru kwa hatia. 29 Lakini kama ng'ombe alikuwa na tabia ya kupiga hapo
awali, na mmiliki wake alionywa lakini hakumzuia, na ng'ombe ameua mwanaume
au mwanamke, huyo ng'ombe lazima apigwe mawe, na mmiliki wake lazima auawe
pia. 30 Kama malipo ya uhai yanaitajika, lazima alipe chochote anachotakiwa kulipa.
31 Kama ng'ombe amempiga mwana wa mwanaume au binti wake, mmiliki wa
ng'ombe anapaswa kufanya kama masharti yanavyo mlazimu. 32 Kama ng'ombe
akimpiga mtumishi wa kiume au wakike, mmiliki wa ngombe lazima alipe shekeli
thelathini za fedha, na ng'ombe lazima apigwe mawe. 33 Kama mwanaume akifungua
shimo, au kama mwanume akichimba shimo na asifunike, na ng'ombe au punda
akaanguka ndani, 34 mmiliki wa shimo lazima alipe madhara. Lazima atoe hela
kwa mmiliki wa mnyama aliye kufa, na mnyama aliye kufa atakuwa wake. 35 Kama
ng'ombe wa mwanaume akimuumiza ng'ombe wa mwanume mwengine hadi kufa,
kisha lazima wamuuze ng'ombe aliye hai na kugawana gharama, na pia lazima
wagawane ng'ombe aliye kufa. 36 Lakini kama ilijulikana kama ng'ombe alikuwa
na tabia ya kupiga hapo awali, na mmiliki wake hakumfunga ndani, hakika lazima
alipe ng'ombe kwa ng'ombe, na mnyama aliye kufa atakuwa wake.

# 22

1 Kama mwanaume akiiba ng'ombe aua kondoo na kumuua au kumuuza, kisha
lazima alipe ng'ombe watano au ng'ombe mmoja, na kondoo wanne kwa mmoja.
2 Kama mwizi akikutwa anavunja ndani, na kama akipigwa na kufa, hakutakuwa
na hatia ya mauaji hayatakuwa juu ya mtu yeyote. 3 Lakini kama jua limechomoza
kabla ya yeye kuvunja ndani, hatia ya mauaji itakuwa juu ya aliyemuua. Mwizi
lazima afanya alipe alichoiba. Kama hana chochote, kisha lazima auzwe kwa uwizi
wake. 4 Kama mnyama amekutwa hai eneo lake, kama ni ng'ombe, punda, au kondoo,
lazima alipe mara mbili. 5 Kama mwanaume akiwapeleka malishoni mifugo yake au
shamba la mizabibu na akawaachia wanyama wake, na kawa wanakula shambani
mwa mwanaume mwengine, lazima afanye malipo bora kutoka shambani mwake
na shamba lake la mizabibu. 6 Kama moto ukitokea na kusambaa kwenye miba hadi
mbegu, au mimea, au shamba kuteketezwa, yeye aliye anzisha moto lazima afanye
malipo. 7 Kama mwanaume akitoa pesa au mali kwa jirani yake amtunzie, na kama
itaibiwa nyumbani mwa huyo mwanaume, kama mwizi akipatikana, huyo mwizi

lazima alipe mara mbili. [8] Lakini kama mwizi asipo patikana, kisha mmiliki wa
nyumba ata kuja mbele za waamuzi kuona kama ameeka mkono wake kwenye mali
za jirani yake. [9] Kwa kila lumbano kuhusu jambo, kama ni ng'ombe, punda, kondoo,
nguo, au chochote kilichopotea mtu anacho sema, “Hichi ni changu,” malalamiko
ya pande zote lazima zije kwa waamuzi. Mwanaume ambaye waamuzi wanamkuta
na hatia ata lipa mara mbili kwa jirani yake. [10] Kama mwanaume akimpa jirani
yake punda, ng'ombe, kondoo, au mnyama yeyote kumuhifadhia, na kama akifa au
kuumia au akibebwa pasipo mtu kumuona, [11] kiapo kwa Yahweh lazima wafanye
wote wawili, kama ndio au hapana mtu ameeka mkono wake kwenye mali ya jirani
yake. Mmiliki lazima akubali hili, na mwengine hatafanya malipo. [12] Lakini kama
iliibwa kwake, mwengine lazima afanye malipo kwa mmiliki kwa ajili yake. [13] Kama
mnyama alikatwa vipande, acha mwanaume mwengine alete huyo mnyama kama
ushahidi. Hatalipa kwa ajili ya vile vipande. [14] Kama mwanaume akiazima mnyama
kutoka kwa jirani yake na mnyama akajeruhia au akafa pasipo mmiliki kuwa naye,
mwanaume mwengine lazima afanya malipo. [15] Lakini kama mmiliki alikuwa
nae, mwanaume mwengine haitaji kulipa; kama mnyama aliazimwa, atalipwa
kwa gharama ya kuazima. [16] Kama mwanaume akimtongoza bikra ambaye hana
mchumba, na kama akilala naye, lazima amfanye kuwa mke wake kwa kulipa
gharama za bibi arusi zinazo stahili. [17] Kama baba yake akikataa kabisa kumpatia,
lazima alipe hela inayo lingana na gharama za bibi arusi bikra. [18] Hautamwacha
mchawi kuishi. [19] Yeyote atakaye lala na mnyama lazima auawe. [20] Yeyote atakaye
toa dhabihu kwa mungu mwengine isipo kuwa Yahweh lazima auawe. [21] Hauta
mkosea mgeni au kumnyanyasa, kwa kuwa ninyi mlikuwa wageni katika nchi ya
Misri. [22] Hauruhusiwi kumtendea vibaya mjane au mtoto asiye kuwa na baba.
[23] Ukiwadhuru ata kidogo, na kama wakiniita mimi, hakika nitasikia sauti yao.
[24] Hasira yangu itawaka, na nitakuua kwa upanga; wake zenu watakuwa wajane,
na watoto wenu pasipo baba. [25] Ukiazima hela kwa watu wangu walio maskini,
haupaswi kuwa kama anaye kopesha hela kwake au kutoza faida. [26] Ukichukuwa
vazi la jirani yako kwa deni, lazima umrudishie kabla jua kuzama, [27] kwa kuwa
hilo ndilo funiko lake, ni vazi la mwili wake. Nini tena ambacho anaweza kulalia?
Atakapo niita mimi, nitasikia, kwa kuwa mimi ni mwenye huruma. [28] Usinikufuru
mimi, Mungu, wala kumtukana mtawala wa watu wako. [29] Husizuie sadaka kutoka
kwenye mavuno yako au kwenye hifadhi ya mvinyo wako. Lazima unipe mzaliwa
wa kwanza wa wana wako. [30] Lazima ufanye hivyo hivyo kwa ng'ombe na kondoo
wako. Kwa siku saba lazima wabaki na mama zao, lakini siku ya nane lazima unipe
mimi. [31] Mtakuwa watu walio tengwa kwa ajili yangu. Hivyo hamtakula nyama iliyo
uliwa na wanyama porini. Badala yake, uwatupie mbwa.

# 23

[1] Haupaswi kutoa taarifa ya uongo kuhusu yeyote. usijiunge na mwanaume muovu
kuwa shahidi wa uongo. [2] Haupaswi kufuata umati kufanya uovu, wala kutoa
ushahidi ukiwa na umati ili kupotosha haki. [3] Haupaswi kumpendelea mwanaume
maskini kwenye kesi yake. [4] Ukikutana na ng'ombe wa adui wako au punda wake
amepotea, lazima umrudishie. [5] Ukiona punda wa yule anaye kuchukia ameanguka
chini na mzigo wake, hauta muacha huyo mtu. Lazima umsaidie na punda wake
[6] Haupaswi kupotosha haki kama yapaswa kwenda kwa watu maskini katika kesi
ya mwanaume maskini. [7] Usijiunge na wengine kufanya shutuma za uongo, na
usiue asiye na hatia wala mwenye haki, kwa kuwa sitamuacha muovu. [8] Husiwai
chukuwa rushwa, kwa kuwa rushwa inawapofusha wanaoona, na kupotosha maneno
ya wakweli. [9] Haupaswi kumnyanyasa mgeni, kwa kuwa wewe ulikuwa mgeni katika

nchi ya Misri. 10 Kwa miaka sita utapanda mbegu kwenye nchi yako na kukusanya
mazao yake. 11 Lakini katika mwezi wa saba utaacha hakujalimwa, ili kwamba
maskini miongoni mwenu wale. Wanacho acha, wanyama wa porini watakula.
Utafanya hivyo na mashamba yenu ya mizabibu na ya mizaituni. 12 Wakati wa
siku sita utafanya kazi, lakini siku ta saba utapumzika. Fanya hivi ili ng'ombe
na punda wako wapumzike, na ili wana wa watumwa wako wa kike na wageni
wapumzike na kupata hauweni. 13 Kuwa makini kwa kila kitu nilicho kwambia.
Husitaje majina ya miungu mingine, wala kuruhusu majina yao kusikika kutoka
mdomoni mwako. 14 Lazima usafiri kusherehekea mara tatu kwa ajili yangu kila
mwaka. 15 Lazima uadhimishe sherehe ya Mkate usiotiwa Chachu. Kama nilivyo
kuamuru, utakula mkate usiotiwa chachu kwa siku saba. Wakati huo, utajitokeza
kwangu mwezi wa Abibu, uliowekwa kwa ajili ya kusudi hili. Ni kwa mwezi huu
uliyo toka Misri. Lakini usijitokeze kwangu mikono mitupu. 16 Lazima uadhimishe
Sherehe ya Mavuno, matunda ya kwanza ya kazi yako ulipo panda mbegu shambani.
Pia lazima uadhimishe Sherehe ya Ukusanyaji wa mwisho wa mwaka, unapo kusanya
mazao yako kutoka shambani. 17 Wanaume wote wako lazima wajitokeze kwa Bwana
Yahweh mara tatu kila mwaka. 18 Haupaswi kutoa damu iliyo tolewa dhabihu
kwangu na mkate uliyotiwa hamira. Mafuta kutoka kwa dhabihu za sherehe zangu
hayapaswi kubaki usiku wote mpaka asubui. 19 Lazima ulete matunda ya kwanza
bora kutoka shambani mwako ndani ya nyumba yangu, nyumba ya Yahweh Mungu
wako. Haupaswi kumchemsha mbuzi mtoto akiwa bado ananyonya. 20 Ninaenda
kumleta malaika mbele yako kukuongoza njiani, na kukuleta sehemu niliyo iandaa.
21 Kuwa makini naye na kumtii. 22 Husimkasirishe, kwa kuwa hatasamehe makosa
yako. Jina langu liko kwake. Kama hakika ukimtii sauti yake na kufanya kila
ninacho kwambia, kisha nitakuwa adui kwa adui zako na mpinzani kwa wapinzani
wako. 23 Malaika mwangu ataenda mbele zako na kukuleta kwa Waamori, Wahiti,
Waperizi, Wakanani, Wahivi, na Wayebusi. Nitawaharibu. 24 Haupaswi kuinamia
miungu yao, kuabudu, au kufanya wanavyo fanya. Badala yake, lazima uwapindue
kabisa na kuvunja nguzo zao za mawe vipande vipande. 25 Lazima umuabudu
Yahweh Mungu wako, na atabariki mkate wako na maji. Nitaondoa magonjwa
miongoni mwenu. 26 Hakuna mwanamke atakaye kuwa tasa au mimba kuharibika
katika nchi yako. Nitawapa maisha marefu. 27 Nitatuma hofu yangu kwao ambao
mnaenda. Nitaua wote mnao kutana nao. Nitafanya maadui zenu wawaogope kwa
kugeuza migongo yao kwenu. 28 Nitatuma mavu kwenu watakao fukuza Wahivi,
Wakanani, na Wahiti mbele zenu. 29 Sitawaondoa kwenu kwa mwaka mmoja, au nchi
itakuwa imetelekezwa, na wanyama wa porini watakuwa wengi kwenu. 30 Badala
yake, nitawafukuza kidogo kidogo kutoka kwenu mpaka utakapo kuwa umestawi na
kurithi nchi. 31 Nitatengeneza mipaka yako kutoka Bahari ya Shamu hadi Bahari ya
Wafilisti, na kutoka nyikani hadi Mto Frati. Nitakupa ushindi juu ya wakazi wote wa
nchi. Utawaondoa kutoka kwako mwenyewe. 32 Haupaswi kufanya agano na wao au
na miungu yao. 33 Hawapaswi kuishi nchini mwako, au watakufanya ufanya dhambi
dhidi yangu. Ukiabudu miungu yao, hakika watakuwa mtego kwako.'"

# 24

1 Kisha Yahweh akamwabia Musa, "Njoo juu kwangu -wewe, Aruni, Nadabu, Abihu,
na wazee sabini wa Israeli, na kuniabudu kwa mbali. 2 Musa peke yake anaweza
kuja karibu yangu. Wengine hawapaswi kuja karibu, wala watu kuja juu na yeye."
3 Musa akaenda juu na kuwaambia watu maneno yote ya Yahweh na amri zake. Watu
wote wakajibu kwa sauti moja na kusema, "Tutafanya maneno yote Yahweh aliyo
tuamuru." 4 Kisha Musa akaandika chini maneno yote ya Yahweh. Asubui mapema,

Musa akajenga madhabahu chini ya mguu wa mlima na kupanga nguzo kumi na
mbili za mawe, ili mawe yawakilishe makabila kumi na mbili ya Israeli. 5 Aliwatuma
vijana Wakiisraeli kutoa sadaka ya kuteketeza na kutoa dhabihu za ng'ombe za
sadaka ya ushirika kwa Yahweh. 6 Musa allichukuwa nusu ya damu na kuweka
kwenye mabeseni; alinyunyuzia nusu ingine kwenye madhabahu. 7 Alichukuwa
kitabu cha agano na kuwasomea kwa nguvu watu. Walisema, “Tutafanya yote
Yahweh aliyo sema. Tutakuwa watiifu.” 8 Kisha Musa akachukuwa damu na
kunyunyiza kwa watu. Alisema, “Hii ni damu ya agano Yahweh alilo lifanya nanyi
kwa kuwapa hii ahadi kwa maneno yote haya.” 9 Kisha Musa, Aruni, Nadabu,
Abihu, na wazee sabini wa Israeli wakaenda juu ya mlima. 10 Walimuona Mungu
wa Israeli. 11 Chini ya miguu yake kulikuwa na sakafu iliyo jengwa kwa jiwe
la yakuti samawi, safi kama mbingu yenyewe. Mungu hakugusa na mkono kwa
hasira viongozi Waisraeli. Walimuona Mungu, na wakanywa na kula. 12 Yahweh
akamwambia Musa, “Njoo juu kwangu mlimani na ubaki pale. Nitakupa saani za
mawe na sheria na amri nilizo ziandika, ili uwafundishe.” 13 Hivyo Musa akaenda
na msaidizi wake Yoshua na kwenda juu mlima wa Mungu. 14 Musa akawaambia
wazee, “Baki hapa na mtusubiri hadi tutakapo warudia. Aruni na Huri wapo nanyi.
Kama kuna mtu mwenye malalamiko, acha awaende.” 15 Hivyo Musa akaenda juu ya
mlima, na wingu likafunika. 16 Utukufu wa Yahweh ukabaki juu ya Mlima wa Sinai,
na wingu likafunika kwa siku sita. Siku ya saba alimuita Musa kutoka ndani ya
wingu. 17 Utukufu wa Yahweh ulikuwa kama moto ulao juu ya mlima kwenye macho
ya Waisraeli. 18 Musa akaingia kwenye wingu na kwenda juu ya mlima. Alikuwa
mlimani siku arobaini na usiku arobaini.

# 25

1 Yahweh akamwambia Musa, 2 “Waambie Waisraeli wanitolee sadaka kila mtu
nawe utapokea kutoka kwa mtu yeyote atakayetoa kwa moyo mkunjufu. Lazima
upokee hizi sadaka kwa ajili yangu. 3 Hizi ndio sadaka utakazopokea kwao; dhahabu,
fedha na shaba, 4 buluu, zambarau na nyekundu, na nguo za kitani safi, na manyoya
ya mbuzi; 5 na ngozi za kondoo dume zilizotiwa rangi nyekundu na ngozi za pomboo,
miti ya mjohoro, 6 mafuta ya ile taa, na viungo vya manukato kwa yale mafuta ya
kupaka na kwa ule uvumba wenye harufu nzuri; 7 mawe ya shohamu na mawe
mengine ya kutiwa kwa ile naivera na kwa kile kifuko cha kifuani. 8 Waache
wanifanyie patakatifu ili nipate kukaa kati yao. 9 Lazima ufanye sawa na haya
yote nikuoneshayo mfano wa maskani, na vifaa vyake, ndivyo utakavyovifanya.
10 Wana paswa wafanye sanduku la mti wa mjohoro. Urefu wake na uwe dhiraa
mbili na nusu; na upana wake moja na nusu, na kwenda juu kwake dhiraa moja na
nusu. 11 Lazima ulifunike nadni kwa dhahabu safi, na utie na ukingo wa dhahabu
kulizunguka pande zote. 12 Nawe uta yayusha katika viduara vinne vya dhahabu,
na kuviweka katika miguu yake minne; viduara viwili upande mmoja, na viduara
viwili upande wake wa pili. 13 Nawe lazima ufanya miti mirefu ya mshita na
kuifunika dhahabu. 14 Nawe lazima uweka hiyo miti katika vile viduara vilivyo katika
pande mbili za sanduku ili kulichukua hilo sanduku. 15 Hiyo miti itakaa katika vile
viduara vya sanduku; haitaondolewa. 16 Kisha weka ndani ya sanduku hizo amri
nitakazokupa. 17 Nawe lazima utengeneze kifuniko cha dhahabu safi. Urefu wake
utakuwa dhiraa mbili na nusu, na upana wake dhiraa moja na nusu. 18 Nawe fanya
makerubi mawili ya dhahabu katika hiyo miisho miwili ya kiti cha rehema. 19 Weka
kerubi moja mwisho mmoja wa kiti cha rehema, na kerubi la pili mwisho wa pili.
Lazima hao makerubi wawe kitu kimoja na kiti cha rehema. 20 Na hao makerubi
watainua mabawa yao juu, na kukifunika hicho kiti cha rehema kwa mabawa

yao. Nyuso zao makerubi zitaelekeana na zitaelekea kiti cha rehema. 21 Lazima
uweke kiti cha rehema juu ya hilo sanduku, kisha uwe hizo amri nitakazokupa
ndani ya sanduku. 22 Nami nitaonana nawe hapo katika sanduku. Nitazungumza
nawe pale nilipo juu ya kiti cha rehema. Itakuwa katikati ya hao makerubi mawili
waliyo juu ya sanduku la ushuhuda nitakapo zungumza na wewe katika mambo yote
nitakayokuagiza kwa ajili ya wana wa Israeli. 23 Nawe fanya meza ya mti wa mshiti.
Urefu wake utakuwa dhiraa mbili, na upana wake dhiraa moja, na kwenda juu kwake
dhiraa moja na nusu. 24 Uifunike dhahabu safi na kuifanyia ukingo wa dhahabu wa
kuizunguka pande zote. 25 Lazima ufanyie fremu ya kuizunguka pande zote, upana
wake utakuwa nyanda nne, ukingo wa dhahabu wa kuuzunguka fremu pande zote.
26 Uifanyie viduara vinne vya dhahabu na kuvitia vile viduara katika pembe zake
nne, katika miguu yake minne ilipo kuwa. 27 Vile viduara na viwe karibu na ile
fremu ili viwe mahali pa kutilia ile miti, ya kuichukulia meza. 28 Fanya ile miti ya
mti wa mshita, na kuifunika dhahabu, kwamba ile meza ichukuliwe kwayo. 29 Nawe
fanya sahani zake, na miiko yake, na makopo yake, na vikombe vyake vya kumiminia.
Vifanye vyote vya dhahabu safi. 30 Nawe utaiweka mikate ya wonyesho juu ya meza
mbele yangu daima. 31 Nawe fanya kinara cha taa cha dhahabu safi; hicho kinara na
kifanywe cha kazi ya kufua, kitako chake, na mti wake, vikombe vyake, na matovu
yake, na maua yake, vyote vitakuwa vya kitu kimoja nacho. 32 Nacho kitakuwa na
matawi sita yenye kutoka ubavuni mwake - matawi matatu ya kinara upande wake
mmoja, na matawi matatu ya kinara upande wake wa pili. 33 Tawi la kwanza lazima
liwe na vikombe vitatu vilivyotengenezwa mfano wa maua ya mlozi katika tawi moja,
tovu na ua na vikombe vitatu vilivyofanywa mfano wa maua ya mlozi katika tawi
la pili, tovu na ua. Vivyo hivyo hayo matawi yote sita yatokayo katika kile kinara.
34 Katika hicho kinara, lazima kuwe na vikombe vinne vilivyofanywa mfano wa maua
ya mlozi, matovu yake, na maua yake. 35 Lazima kuwe na tovu chini ya matawi -
mawili la kitu kimoja nacho, na tovu chini ya matawi mawili la kitu kimoja nacho,
na tovu chini ya matawi mawili la kitu kimoja nacho, kwa hayo matawi sita yatokayo
katika kile kinara. 36 Matovu yake na matawi yake yatakuwa ya kitu kimoja nacho,
kiwe chote pia kazi moja ya kufua, ya dhahabu safi. 37 Lazima nawe uzifanye hivyo
vinara saba na taa zake saba, nao wataziwasha hizo taa zake, zitoe nuru mbele yake.
38 Na makoleo yake, na visahani vyake, vyote vitakuwa vya dhahabu safi. 39 Tumia
talanta moja ya dhahabu safi, pamoja na vyombo hivi vyote. 40 Nawe angalia ya
kwamba uvifanye kama mfano wake, uliooneshwa mlimani.

# 26

1 Lazima ufanye hiyo maskani iwe na mapazia kumi ifanye ya nguo ya kitani nzuri
ya kusokota, pamoja na nyuzi za rangi ya buluu, zambarau na nyekundu, pamoja
na makerubi. Kazi ya fundi stadi. 2 Urefu wa kila pazia utakuwa dhiraa ishirini
na nane, na upana wa kila pazia utakuwa dhiraa nne. Mapazia yote yatakuwa ya
kipimo kimoja. 3 Mapazia matano yataungwa pamoja, na mapazia matano mengine
yataungwa pamoja. 4 Lazima ufanye tanzi za rangi ya samawati upande wa mwisho
wa pazia moja katika ule upindo wa fungu lake. Vivyo hivyo utafanya upande wa
mwisho wa ile pazia iliyo, katika fungu la pili. 5 Fanya matanzi hamsini katika
pazia moja, na matanzi hamsini katika upande wa mwisho wa ile pazia iliyo katika
kuungana kwa pili. 6 Fanya hivi ili hizo tanzi zielekeana. Kisha ufanye vifungo
hamsini vya dhahabu, na kuunganisha hayo mapazia pamoja kwa vile vifungo na
hiyo maskani itakuwa ni moja. 7 Lazima ufanye mapazia ya nywele za mbuzi
yawe hema juu ya maskani. Lazima ufanye mapazia kumi na moja. 8 Urefu wa
kila pazia utakuwa dhiraa thelathini, na upana wa kila pazia utakuwa dhiraa nne.

Hayo mapazia kumi na moja yatakuwa ya kipimo kimoja. 9 Lazima utaunganisha
mapazia matano mbali, na mapazia sita mbali, na lile pazia la sita utalikunja hapo
upande wa mbele wa ile hema. 10 Ufanye tanzi hamsini upande wa mwisho wa
pazia lile lililo la mwisho katika hayo yaliyounganywa pamoja, na tanzi hamsini
upande wa mwisho wa lile pazia lililo nje katika hayo ya pili yaliyounganywa pamoja.
11 Kisha ufanye vifungo hamsini vya shaba, na kuvitia vile vifungo katika zile tanzi,
na kuiunganya ile hema pamoja, ili iwe hema moja. 12 Kipande kile kilichosalia,
kile kiangukacho, cha yale mapazia ya hema, itaanguka huko upande wa nyuma
wa maskani. 13 Lazima kuwe na dhiraa moja upande mmoja, na ile dhiraa moja
upande wa pili - ya urefu wa mapazia ya hema uliosalia, zitaanguka katika ubavu
wa maskani upande huu na upande huu, ili kuifunika. 14 Nawe fanya kifuniko cha
ile hema, cha ngozi za kondoo dume zilizotiwa rangi nyekundu, na juu yake kifuniko
cha ngozi za pomboo. 15 Nawe lazima ufanye hizo fremu za maskani za mti wa
mjohoro. 16 Kila fremu utakuwa na urefu wa dhiraa kumi, na upana wake kila
ubao utakuwa dhiraa moja na nusu. 17 Kila fremu itakuwa na ndimi mbili, zenye
kuunganishwa huu na huu. Ndivyo utakavyozifanya mbao zote za maskani. 18 Kisha
ufanye zile mbao za maskani, mbao ishirini kwa upande wa kusini kuelekea kusini.
19 Lazima nawe ufanye vitako arubaini vya fedha chini ya zile fremu ishirini. Vitako
viwili chini ya fremu moja, kupokea zile ndimi zake mbili, na vitako viwili chini ya
fremu nyingine kupokea zile ndimi zake mbili. 20 Kwa upande wa pili wa maskani,
upande wa kaskazini, mbao ishirini 21 na vitako vyake vya fedha arubaini. Lazima
kuwe na vitako viwili chini ya fremu moja, na vitako viwili chini ya fremu nyingine.
22 Ufanye fremu sita kwa ajili ya upande wa nyuma wa maskani kuelekea magharibi.
23 Tena ufanye fremu mbili kwa ajili ya hizo pembe za maskani zilizo upande wa
nyuma. 24 Hizi fremu zitakuwa zimetengana upande wa chini, lakini zimeshinkana
kwa juu ya duara moja. 25 Fremu zitakuwa ni nane, na vitako vyake vya fedha. Vitako
kumi na sita, vitako viwili chini ya fremu moja, na vitako viwili chini ya ubao wa
pili. 26 Lazima ufanye mataruma ya mti wa mshita- mataruma matano kwa ajili ya
mbao za upande mmoja wa maskani, 27 na mataruma matano kwa ajili ya fremu za
upande wa pili wa maskani, na mataruma matano kwa ajili ya fremu za upande wa
maskani ulio nyuma kuelekea magharibi. 28 Na hilo taruma la katikati lililo katikati
ya zile fremu, litapenya toka mwisho huu hata mwisho huu. 29 lazima uzifunuke
hizo fremu kwa dhahabu. Nawe lazima ufanye maduara yake ya za dhahabu, kuwa
kama vishikizo, na hayo mataruma utayafunika dhahabu. 30 Nawe utaisimamisha
hiyo maskani sawasawa na mfano wake uliooneshwa mlimani. 31 Nawe fanya pazia
la nyuzi za rangi ya buluu, zambarau na nyekundu, na nguo za kitani nzuri zenye
kusokotwa, litafumwa na kutiwa makerubi, kazi ya fundi stadi. 32 Kisha litungike
katika nguzo nne za mti wa mshita zilizofunikwa dhahabu, vifungo vyake vitakuwa
vya dhahabu, katika vitako vya fedha vinne. 33 Nawe tungika lile pazia chini ya
vile vifungo, nawe lete lile sanduku la ushuhuda. Lile pazia litawagawanyia kati
ya patakatifu, na mahali patakatifu sana. 34 Nawe lazima utaweka kiti cha rehema
juu ya lile sanduku la ushuhuda ndani ya mahali pale patakatifu sana. Na ile meza
utaiweka nje ya pazia. 35 Lazima uweke kinara cha taa kuikabili ile meza upande
wa maskani wa kuelekea kusini. Lile meza utaiweka upande wa kaskazini. 36 Kisha
utafanya kisitiri kwa mlango wa hema, cha nyuzi za rangi ya buluu, zambarau, na
nyekundu, na kitani nzuri yenye kusokotwa, kazi ya mshonaji wa taraza. 37 Nawe
fanya nguzo tano za mti wa mshita kwa kile kisitiri, na kuzifunika dhahabu; kulabu
zake zitakuwa za dhahabu. Nawe utasubu vitako vya shaba vitano kwa ajili yake.

# 27

[1] Nawe fanya madhabahu ya mti wa mshita, urefu wake utakuwa ni dhiraa tano
na upana wake dhiraa tano. Hiyo madhabahu itakuwa mraba na kwenda juu kwake
kutakuwa dhiraa tatu. [2] Nawe fanya pembe nne kama mfano wa pembe za ng'ombe.
Hizo pembe zitakuwa za kitu kimoja na madhabahu, nawe utayafunika kwa shaba.
[3] Lazima vyombo vyake vya kuyaondoa majivu yake utavifanya, na majembe yake,
na mabakuli yake, na uma zake, na meko yake. Vyombo vyake vyote utavifanya
vya shaba. [4] Nawe uifanyie hiyo madhabahu wavu wa shaba. Kisha utie pete nne
za shaba katika hizo pembe nne za ule wavu. [5] Nawe lazima uweke huo wavu
chini ya kizingo kiizungukacho madhabahu upande wa chini. [6] Nawe fanya miti
kwa ajili ya madhabahu, miti ya mshita, na kuifunika shaba. [7] Na hiyo miti itatiwa
katika viduara, na ile miti itakuwa katika pande mbili za madhabahu, wakati wa
kuichukua. [8] Uifanye ya mbao, yenye mvungu ndani yake kama ulivyooneshwa
mlimani. [9] Nawe ufanye ua wa maskani. Upande wa kusini wa kuelekea kusini
kutakuwa na chandarua ya nguo ya kitani nzuri yenye kusokotwa, kwa huo ua,
urefu wake upande mmoja utakuwa ni dhiraa mia moja. [10] Na nguzo zake zitakuwa
nguzo ishirini, na vitako vyake ishirini, vitako vyake vitakuwa vya shaba kulabu
za zile nguzo na vitanzi vyake vitakuwa vya fedha. [11] Ni vivyo hivyo upande wa
kaskazini, urefu wake hiyo chandarua utakuwa ni dhiraa mia moja, na nguzo zake
ishirini, na vitako vyake ishirini vitakuwa vya shaba, kulabu za zile nguzo na vitanzi
vyake vitakuwa vya fedha. [12] Na upande wa magharibi, upana wa ua kutakuwa na
chandarua ya dhiraa hamsini; nguzo zake kumi, na vitako vyake kumi. [13] Na upana
wa ule ua upande wa mashariki kuelekea mashariki utakuwa ni dhiraa hamsini.
[14] Chandarua upande mmoja wa lango itakuwa dhiraa kumi na tano upana wake.
Lazima nguzo zake zitakuwa tatu na vitako vyake vitatu. [15] Upande wa pili ni vivyo
hivyo chandarua ya dhiraa kumi na tano; nguzo zake tatu, na vitako vyake vitatu.
[16] Na kwa lile lango la ua patakuwa na kisitiri cha dhiraa ishirini, kitakuwa cha nguo
ya rangi ya buluu, zambarau na nyekundu, na kitani nzuri yenye kusokotwa, kazi
ya mshonaji taraza; nguzo zake zitakuwa nne, na vitako vyake vinne. [17] Nguzo zote
za ule ua ziuzungukao pande zote zitakuwa na vitanzi vya fedha; kulabu zake za
fedha, na vitako vyake vya shaba. [18] Urefu wa huo ua utakuwa dhiraa mia moja, na
upana wake utakuwa dhiraa hamsini kotekote, na kwenda juu kwake dhiraa tano;
yawe ya nguo ya kitani nzuri, na vitako vyake vitakuwa vya shaba. [19] Vyombo vyote
vya maskani vitumiwavyo katika utumishi wake wote, na vigingi vyake vyote, na
vigingi vyote vya ule ua, vitakuwa vya shaba. [20] awe waamuru wana wa Israeli
wakuletee mafuta ya zeituni safi ya kupondwa kwa ajili ya nuru, ili kufanya ile taa
kuwaka daima. [21] Ndani ya ile hema ya kukutania, nje ya hilo pazia, lililo mbele ya
huo ushuhuda, Haruni na wanawe wataitengeza tangu jioni hadi asubuhi mbele ya
BWANA; itakuwa ni amri ya milele katika vizazi vyao vyote kwa ajili ya wana wa
Israeli.

# 28

[1] Umuite Aruni kaka yako na wana wake - Nadabu, na Abihu, na Eleazari, na
Ithamari - miongoni mwa wana wa Israeli, ili anitumikie katika kazi ya ukuhani.
[2] Nawe utamfanyia Aruni ndugu yako mavazi matakatifu, kwa utukufu na kwa
uzuri. [3] Nawe utawaambia watu wote wenye moyo wa hekima, niliowajaza na
roho ya hekima wamfanyie Aruni mavazi ili kumtakasa anitumikie katika kazi ya
ukuhani. [4] Na mavazi watakayoyafanya ni kifuko cha kifuani, na naivera, na joho,
na kanzu ya kazi ya urembo, na kilemba, na mshipi; nao watawafanyia Aruni
nduguye, na wanawe, mavazi matakatifu ili anitumikie katika kazi ya ukuhani. [5] Nao

wataitwaa dhahabu, na nguo ya rangi ya samawi, na ya rangi ya zambarau, na ya
rangi nyekundu. 6 Nao waifanye naivera kwa nyuzi za dhahabu, na za samawi, na
za zambarau, na nyekundu, na kitani nzuri yenye kusokotwa kwa kazi ya mstadi.
7 Lazima itakuwa na vipande viwili vya mabegani, vilivyoungana kwenye ncha zake
mbili; ili ipate kuunganywa. 8 Na mshipi wa kazi ya ustadi ulio juu yake, ili kuifunga
mahali pake; utakuwa wa kazi kama ile ya naivera, ya vitu vile vile ya nyuzi za
dhahabu, na za rangi ya samawi, na ya zambarau, na nyekundu, na kitani nzuri
yenye kusokotwa. 9 Nawe utatwaa vito viwili vya shohamu, ya rangi ya chani-kiwiti,
nawe utachora juu yake majina ya wana wa Israeli; 10 Majina yao sita katika kito
kimoja, na majina sita yaliyosalia katika kile kito cha pili, kwa utaratibu wa kuzaliwa
kwao. 11 Kwa kazi mtu mwenye kuchora mawe kama vile muhuri ichorwavyo,
utavichora hivi vito viwili, sawasawa na majina ya wana wa Israeli, nawe utavitia
katika vijalizo vya dhahabu. 12 Nawe utavitia vile vito viwili juu ya vipande vya
mabegani vya hiyo naivera, viwe vito vya ukumbusho kwa ajili ya wana wa Israeli.
Naye Aruni atayachukua majina yao mbele za Yahweh juu ya mabega yake mawili
ili kuwa ukumbusho. 13 Nawe fanya vijalizo viwili vya dhahabu 14 na mikufu miwili
ya dhahabu safi; utaifanya iwe mfano wa kamba, ya kazi ya kusokotwa; nawe uitie
ile mikufu ya kazi ya kusokotwa katika vile vijalizo. 15 Nawe lazima utafanya kifuko
cha kifuani cha hukumu, kazi ya fundi stadi; utakifanya kwa kuiandama ile kazi
ya hiyo naivera. Fanya nyuzi za dhahabu, na za rangi ya samawi, na za rangi ya
zambarau, na nyekundu, na kitani safi yenye kusokotwa, ndivyo utakavyokifanya.
16 Kitakuwa mraba, tena cha kukunjwa; urefu wake utakuwa shibiri moja, na upana
wake shibiri moja. 17 Nawe ukijaze viweko vya vito, safu nne za vito; safu moja
itakuwa ni akiki, na yakuti ya rangi ya manjano, na baharamani, hivi vitakuwa
safu ya kwanza. 18 Na safu ya pili itakuwa zumaridi, na yakuti samawi, na almasi.
19 Na safu ya tatu itakuwa hiakintho, na akiki nyekundu, na amethisto. 20 Na safu
ya nne itakuwa ni zabarajadi, na shohamu, na yaspi. Vito hivyo vitakazwa ndani
ya dhahabu kwa kujaa mahali pake. 21 Na vile vito vitakuwa sawasawa na majina
ya wana wa Israeli, kumi na viwili, sawasawa na majina yao. Mfano wa kuchora
kwa muhuri kila kimoja sawasawa na jina lake, vitakuwa vya hizo kabila kumi na
mbili. 22 Nawe lazima utie katika kile kifuko cha kifuani mikufu mfano wa kamba,
ya kazi ya kusokotwa, ya dhahabu safi. 23 Nawe utie maduara mawili ya dhahabu
katika kile kifuko cha kifuani, na kuzitia hizo pete mbili katika ncha mbili za kifuko
cha kifuani. 24 Nawe utie hiyo mikufu miwili ya dhahabu iliyosokotwa katika zile
pete mbili zilizo katika ncha za kifuko cha kifuani. 25 Na ncha zile nyingine za hiyo
mikufu miwili ya kusokotwa utazitia katika vile vijalizo viwili, na kuvitia katika vile
vipande vya mabegani vya naivera upande wa mbele. 26 Nawe utafanya viduara vili
vya dhahabu, uzitie katika hizo ncha mbili za kifuko cha kifuani, katika ukingo wake.
27 Nawe lazima ufanye viduara vili vya dhahabu, na kuzitia katika vile vipande viwili
vya mabegani vya ile naivera chini yake, upande wa mbele, karibu na kifungo chake,
juu ya huo mshipi wa naivera uliosukwa kwa ustadi. 28 Nao watakikaza kile kileso
kwa vile viduara vyake kwenye viduara za naivera kwa ukanda wa rangi ya samawi,
ili kwamba kikae pale juu ya ule mshipi wa naivera uliosukwa kwa ustadi, ili kwamba
kifuko cha kifuani kisiachane na naivera. 29 Na Aruni atayachukua majina ya wana
wa Israeli katika kile kifuko cha kifuani cha hukumu juu ya moyo wake kwa kufanya
maamuzi, hapo atakapoingia ndani ya mahali patakatifu, kuwa ukumbusho mbele
yaYahweh daima. 30 Nawe utie hizo Urimu na Thumimu katika kile kifuko cha kifuani
cha hukumu; nazo zitakuwa juu ya moyo wa Aruni, hapo atakapoingia ndani mbele
ya Yahweh na Aruni atachukua hukumu ya hao wana wa Israeli juu ya moyo wake
mbele ya Yahweh daima. 31 Nawe fanya hiyo joho ya naivera ya rangi ya samawi yote.

[32] Nayo itakuwa na tundu katikati yake kwa kupitisha kichwa; itakuwa na utepe wa
kazi ya kusokotwa kuzunguka hilo tundu lake, mfano wa tundu lililo katika kanzu
ya chuma, ili lisipasuke. [33] Nawe katika pindo zake utatia makomamanga ya rangi
ya samawi, na ya rangi ya zambarau, na ya rangi nyekundu, kuzunguka pindo zake
kotekote; na njuga za dhahabu kati ya hayo makomamanga pande zote. [34] Kengele ya
dhahabu na komamanga, kengele ya dhahabu na komamanga, katika pindo za joho
kuizunguka pande zote. [35] Nayo itakuwa juu ya Aruni akitumika; na sauti ya hizo
kengele itasikilikana hapo aingiapo ndani ya mahali patakatifu mbele ya Yahweh na
hapo atokapo nje, ili kwamba asife. [36] Nawe fanya bamba la dhahabu safi na kuchora
juu yake, mfano wa machoro ya muhuri, "Mtakatifu kwa Yahweh." [37] Nawe ulitie
hilo bamba katika ukanda wa rangi ya samawi, nalo litakuwa katika kile kilemba;
litakuwa upande wa mbele wa kile kilemba. [38] Nalo litakuwa katika kipaji cha uso
cha Aruni, na Aruni atauchukua uovu wa vile vitu vitakatifu, watakavyovitakasa
hao wana wa Israeli katika vipawa vyao vyote vitakatifu, nalo litakuwa katika kipaji
chake cha uso sikuzote, ili kwamba vipate kukubaliwa mbele za Yahweh. [39] Na hiyo
kanzu utaifuma ya kitani nzuri ya kazi ya urembo, ufanye na kilemba cha nguo
ya kitani nzuri, nawe utafanya mshipi wa kazi ya mwenye kutia taraza. [40] Kisha
utafany kanzu kwa ajili ya wana wa Aruni, nawe wafanyie mishipi, wafanyie na kofia
kwa utukufu na uzuri. [41] Nawe mvike huyo nduguye Aruni na wanawe nao mavazi
hayo; nawe watie mafuta, na kuwaweka kwa kazi takatifu, na kuwatakasa, ili wapate
kunitumikia mimi katika kazi ya ukuhani. [42] Nawe wafanyie suruali za nguo ya kitani,
ili kufunika tupu ya miili yao; suruali hizo zitafika tangu kiunoni hata mapajani.
[43] Aruni na wanawe watazivaa, hapo watakapoingia katika hema ya kukutania, au
hapo watakapoikaribia madhabahu ili watumike katika mahali patakatifu; wasije
wakachukua uovu, wakafa; hii itakuwa ni amri ya milele kwake yeye, na kwa wazao
wake.

# 29

[1] Sasa Hivi ndivyo wapaswa kufanya kuwatenga ili wanitumikie kama makuhani.
Chukuwa mtoto wa ng'ombe dume na kondoo bila lawama, [2] mkate bila hamira, na
keki bila hamira iliyo changanywa na mafuta. Pia chukuwa maandazi bila hamira
yalio pakwa mafuta. Fanya maandazi kwa unga mzuri wa ngano. [3] Lazima uweke
kwenye ndoo moja, leta kwenye ndoo, na kuleta pamoja na ng'ombe dume na
wana kondoo wawili. [4] Lazima nawe umlete Aruni na wana wake wawili katika
lango la kuingilia hema la kukutania. Lazima uwasafishe Aruni na wana wake
kwenye maji. [5] Kisha twaa hayo mavazi na kumvika Haruni; itie kanzu, na joho
ya naivera, na naivera, na kifuko cha kifuani, na kumkaza kwa huo mshipi wa
naivera uliosukwa kwa ustadi. [6] Nawe mvike kile kilemba kichwani, na ile taji
takatifu utaitia katika kile kilemba. [7] Ndipo utakapotwaa hayo mafuta ya kutiwa,
na kummiminia kichwani mwake, na kumtia mafuta. [8] Kisha walete hao wanawe
na kuwavika kanzu. [9] Nawe uwakaze mishipi, Aruni na wanawe, na kuwavika
kofia. Nao watakuwa na huo ukuhani kwa amri ya milele. Nawe utawaweka Haruni
na wanawe kwa kazi takatifu. [10] Kisha utamleta huyo ng'ombe mbele ya hema
ya kukutania; na Haruni na wanawe wataweka mikono yao juu ya kichwa cha
huyo ng'ombe. [11] Kisha utamchinja huyo ng'ombe mbele ya Yahweh pa hema ya
kukutania. BWANA, [12] Kisha twaa baadhi ya damu ya ng'ombe, uitie katika pembe
za madhabahu kwa kidole chako; na kuimimina damu yote chini ya madhabahu.
[13] Kisha chukuwa mafuta yote yafunikayo matumbo, na kitambi kilicho katika ini, na
figo mbili, na mafuta yaliyo juu yake, uyateketeze yote juu ya madhabahu. [14] Lakini
nyama yake huyo ng'ombe, na ngozi yake, na mavi yake, utayachoma kwa moto nje

ya marago; ni sadaka kwa ajili ya dhambi. [15] Pia mtwae kondoo mume mmoja; na
Aruni na wanawe wataweka mikono yao juu ya kichwa chake huyo kondoo mume.
[16] Kisha utamchinja huyo kondoo mume, na kuitwaa damu yake, na kuinyunyiza
katika madhabahu kuizunguka kando-kando. [17] Kisha utamkata-kata kondoo vipande
vyake, na kuyaosha matumbo yake na miguu yake, na kuiweka pamoja na vipande
vyake na kichwa chake, [18] nawe mteketeze kondoo mzima juu ya madhabahu. Ni
sadaka ya kuteketezwa kwa ajili yaYahweh; ni harufu nzuri, sadaka iliyosongezwa
kwa Yahweh kwa njia ya moto. [19] Kisha mtwae huyo kondoo mwingine; na Aruni
na wanawe wataweka mikono yao juu ya kichwa chake huyo kondoo. [20] Kisha
utamchinja kondoo, na kuitwaa damu yake, na kuitia katika ncha ya sikio la Aruni
la upande wa kuume, na katika ncha za masikio ya kuume ya wanawe, na katika
vyanda vya gumba vya mikono yao ya kuume, na katika vidole vikuu vya miguu
yao ya kuume, na kuinyunyiza hiyo damu katika madhabahu kuizunguka kando-
kando. [21] Kisha twaa katika hiyo damu iliyo juu ya madhabahu, na katika hayo
mafuta ya kutiwa, na kumnyunyizia Aruni, juu ya mavazi yake, na wanawe, na
mavazi yao pia, pamoja naye; naye atatakaswa, na mavazi yake, na wanawe, na
mavazi ya wanawe, pamoja naye. [22] Tena yatwae mafuta ya huyo kondoo mume, na
mkia wake wa mafuta, na mafuta yafunikayo matumbo, na kitambi kilicho katika
ini, na figo mbili, na mafuta yaliyo katika hizo figo, na paja la kuume; kwani ni
kondoo ambaye ni wa kuwekwa kwa kazi takatifu. [23] Utwae na mkate mmoja wa
unga, na mkate mmoja ulioandaliwa kwa mafuta, na kaki moja katika kile kikapu
cha mikate isiyotiwa chachu, kilichowekwa mbele ya Yahweh. [24] Nawe utavitia hivi
vyote katika mikono ya Aruni, na katika mikono ya wanawe; nawe utavitikisa-tikisa
viwe sadaka ya kutikiswa mbele za Yahweh. [25] Kisha uvitwae vile vitu mikononi
mwao, na kuviteketeza juu ya madhabahu, juu ya ile sadaka ya kuteketezwa, viwe
harufu nzuri mbele yangu; ni sadaka iliyotengenezwa kwangu kwa njia ya moto.
[26] Kisha twaa kidari cha huyo kondoo wa kuwekwa kwake Haruni kwa kazi takatifu,
na kukitikisa-tikisa kiwe sadaka ya kutikiswa mbele za Yahwe nacho kitakuwa ni
sehemu yako. [27] Nawe kitakase kile kidari cha ile sadaka ya kutikiswa, na lile paja la
sadaka ya kuinuliwa, lililotikiswa, na lililoinuliwa juu, vya yule kondoo wa kuwekwa
kwa kazi takatifu, huyo aliyekuwa kwa ajili ya Aruni na wanawe. [28] Navyo vitakuwa
vya Haruni na wanawe posho ya lazima sikuzote itokayo kwa hao wana wa Israeli;
kwa kuwa ni sadaka ya kuinuliwa; nayo itakuwa ni sadaka ya kuinuliwa itokayo
kwa hao wana wa Israeli katika dhabihu zao za sadaka za amani, ni sadaka yao ya
kuinuliwa kwa ajili ya Yahweh. [29] Na hayo mavazi matakatifu ya Aruni yatakuwa ya
wanawe baada yake, wayavae watakapotiwa mafuta, na watakapowekwa kwa kazi
takatifu. [30] Huyo mwanawe atakayekuwa kuhani badala yake atayavaa muda wa
siku saba, hapo atakapoingia ndani ya hiyo hema ya kukutania, ili atumike ndani
ya mahali patakatifu. [31] Nawe twaa huyo kondoo mume aliyekuwa wa kuwekwa
kwa kazi takatifu, na kuitokosa nyama yake katika mahali patakatifu. [32] Na Aruni na
wanawe wataila ile nyama ya kondoo, na mikate iliyo katika kile kikapu, hapo mbele
ya mlango wa hema ya kukutania. [33] Nao watakula vile vitu ambavyo upatanisho
ulifanywa kwa hivyo, ili kuwaweka kwa kazi takatifu na kuwatakasa; lakini mgeni
asivile, maana, ni vitu vitakatifu. [34] Na kwamba kitu cho chote cha ile nyama,
iliyo kwa ajili ya kuweka kwa kazi takatifu, au cho chote cha hiyo mikate, kikisalia
hata asubuhi, ndipo utavichoma kwa moto hivyo vilivyosalia; havitaliwa, maana,
ni vitu vitakatifu [35] Ni hivyo utakavyowatendea Aruni na wanawe kama nilivyo
kuagiza. Utawaweka kwa kazi takatifu siku saba. [36] Kila siku utamtoa ng'ombe
wa sadaka ya dhambi kwa ajili ya upatanisho; nawe utaisafisha hiyo madhabahu,
hapo utakapofanya upatanisho kwa ajili ya hiyo madhabahu; nawe utaitia mafuta,

ili kuitakasa. [37] Utafanya upatanisho kwa ajili ya hiyo madhabahu muda wa siku
saba, na kuitakasa; ndipo madhabahu itakapokuwa takatifu sana; kila kitu kiigusacho
madhabahu kitakuwa kitakatifu. [38] Lazima utoe kwenye madhabahu wana-kondoo
wa mwaka mmoja wawili siku baada ya siku [39] daima. Mwana-kondoo mmoja
utamchinja asubuhi; na mwana-kondoo wa pili utamchinja jioni [40] Pamoja na mwana-
kondoo mmoja utatoa vibaba vitatu vya unga mzuri uliochanganyika na mafuta
yenye kupondwa, kiasi cha kibaba na robo kibaba; na divai kiasi cha kibaba na
robo kibaba, iwe sadaka ya kinywaji. [41] Na huyo mwana-kondoo wa pili utamchinja
wakati wa jioni. Nawe utamfanyia vivyo kama ile sadaka ya unga ya asubuhi, na
kama ile sadaka yake ya kinywaji. Hii itatoa harufu nzuri, ni dhabihu ya kusongezwa
kwangu kwa njia ya moto. [42] Itakuwa ni sadaka ya kuteketezwa milele katika
vizazi vyenu vyote mlangoni pa ile hema ya kukutania mbele ya Yahweh, hapo
nitakapokutana nanyi, ili niseme na wewe hapo. [43] Nami nitakutana na wana wa
Israeli hapo; na hiyo hema itafanywa takatifu na utukufu wangu. Nami nitaitakasa
hiyo hema ya kukutania, na hiyo madhabahu. [44] Pia Aruni na wanawe nitawatakasa,
ili wanitumikie katika kazi ya ukuhani. [45] Na mimi nitakaa kati ya wana wa Israeli,
nami nitakuwa Mungu wao. [46] Nao watanijua kuwa mimi ndimi Yahweh, Mungu wao,
niliyewaleta watoke katika nchi ya Misri, nipate kukaa kati yao. Ni mimi Yahweh,
Mungu wao.

# 30

[1] Nawe fanya madhabahu ya kufukizia uvumba; utaifanyiza kwa mti wa mshita.
[2] Urefu wake utakuwa dhiraa moja, na upana wake dhiraa moja; itakuwa mraba; na
kwenda juu kwake dhiraa mbili; pembe zake zitakuwa za kitu kimoja nayo. [3] Nawe
utaifunikiza dhahabu safi juu yake - na mbavu zake kando kando, na pembe zake.
Nawe utaifanyia ukingo wa dhahabu kuizunguka. [4] Kisha utaifanyia pete mbili za
dhahabu, chini ya ukingo wake katika mbavu zake mbili, katika pande zake mbili
utazifanya; nazo zitakuwa mahali pa kuitia miti ya kuichukulia madhabahu. [5] Na ile
miti utaifanya kwa mti wa mshita, na kuifunikiza dhahabu safi. [6] Nawe utaitia mbele
ya lile pazia lililo karibu na sanduku la ushuhuda mbele ya kiti cha rehema kilicho
juu ya ushuhuda, hapo nitakapokutana nawe. [7] Na Aruni atafukiza uvumba wa
manukato juu yake; kila siku asubuhi. Atakapozitengeneza zile taa, ataufukiza, [8] na
Aruni atakapoziwasha zile taa wakati wa jioni, ataufukiza, uwe uvumba wa daima
mbele za Yahweh katika vizazi vyenu vyote. [9] Hamtafukiza juu yake uvumba mgeni,
wala sadaka ya kuteketezwa, wala sadaka ya unga, wala hamtamimina juu yake
sadaka ya kinywaji. [10] Naye Aruni atafanya upatanisho juu ya pembe zake mara moja
kila mwaka. Kwa damu ya ile sadaka ya dhambi ya kufanya upatanisho, mara moja
kila mwaka ataifanyia upatanisho, katika vizazi vyenu vyote. Ni takatifu sana kwa
Yahweh." [11] BWANA akanena na Musa, [12] "Utakapowahesabu wana wa Israeli, kama
itakavyotokea hesabu yao, ndipo watakapompa BWANA kila mtu ukombozi kwa ajili
ya roho yake, hapo utakapowahesabu; ili kwamba yasiwe maradhi kati yao, hapo
utakapowahesabu. [13] Kila mtu apitaye kwa wale waliohesabiwa atatoa nusu shekeli
kwa kuiandama shekeli ya mahali patakatifu; (shekeli ni gera ishirini). Nusu shekeli
kwa sadaka ya Yahweh. [14] Kila mtu apitaye kwa wale waliohesabiwa tangu huyo
ambaye umri wake ni miaka ishirini, au zaidi, atatoa hiyo sadaka kwangu. [15] Watu
watakapo leta hii sadaka kwangu kufanya upatananisho, matajiri hawataleta zaidi,
wala maskini hawataleta kilichopungua katika hiyo nusu shekeli. [16] Nawe utapokea
hizo fedha za upatanisho mikononi mwa hao wana wa Israeli, na kuziweka kwa ajili
ya utumishi wa hema ya kukutania. Ili kwamba ziwe ukumbusho kwa ajili ya wana
wa Israeli mbele yangu ili kufanya upatanisho kwa ajili ya roho zenu. [17] Yahweh

akamwambia Musa, [18] "Fanya na birika la shaba, na tako lake la shaba, ili kuogea;
nawe utaliweka kati ya hema ya kukutania na madhabahu, nawe utalitia maji. [19] Na
Aruni na wanawe wataosha mikono yao na miguu yao humo. [20] Hapo waingiapo
ndani ya hema ya kukutania au waendepo karibu na madhabahu kunitumikia kwa
kuchoma sadaka, watajiosha majini, ili wasife. [21] Basi wataosha mikono yao na miguu
yao ili kwamba wasife; na neno hili litakuwa amri kwao milele, kwake yeye na kwa
wazao wake katika vizazi vyao vyote. [22] Kisha Yahweh akasema na Musa, [23] "Jitwalie
manukato yaliyo bora, manemane mbichi shekeli mia tano, na mdalasini wenye
harufu nzuri 250, na kane shekeli 250 [24] na kida shekeli mia tano, kwa kuiandama
shekeli ya mahali patakatifu, na mafuta ya zeituni kiasi cha vibaba vitano. [25] Nawe
utayafanya mafuta ya kutiwa matakatifu, marhamu iliyochanganywa kwa kazi ya
ustadi ya mtengezaji manukato; yatakuwa ni mafuta matakatifu ya kutiwa. [26] Nawe
utaipaka hema ya kukutania kwa mafuta hayo, na hilo sanduku la ushuhuda, [27] na
hiyo meza, na vyombo vyake vyote, na kinara cha taa, na vyombo vyake, [28] na
madhabahu ya kufukizia uvumba, na madhabahu ya kuteketezea sadaka, pamoja
na vyombo vyake vyote, na birika, na tako lake. [29] Nawe utavitakasa vitu hivyo, ili
viwe vitakatifu sana; tena kila kivigusacho vyombo vile kitakuwa kitakatifu. [30] Nawe
utawatia mafuta Aruni na wanawe, na kuwatakasa, ili wanitumikie katika kazi ya
ukuhani. [31] Nawe utanena na wana wa Israeli na kuwaambia, Haya yatakuwa
ni mafuta matakatifu ya kutiwa kwa ajili yangu mimi katika vizazi vyenu vyote.
[32] Hayatamiminwa katika kiwiliwili cha binadamu, wala msifanye mengine mfano wa
haya kama yalivyoungwa kwa viungo vyake; ni matakatifu, na kwenu ninyi yatakuwa
matakatifu. [33] Mtu awaye yote atakayechanganya mafuta mfano wa haya, au mtu
awaye yote atakayetia mafuta haya juu ya mgeni, mtu huyo atakatiliwa mbali na watu
wake.'" [34] Yahweh akamwambia Musa, "Jitwalie manukato mazuri, yaani, natafi, na
shekelethi, na kelbena; viungo vya manukato vizuri pamoja na ubani safi; vitu hivyo
vyote na viwe vya kipimo kimoja. [35] Nawe utafanya uvumba wa vitu hivyo, manukato
ya kazi ya ustadi wa mtengenazaji manukato, yatakuwa yamekolea, safi, matakatifu.
[36] Nawe baadhi yake utayaponda sana, na kuyaweka mbele ya ushuhuda ndani ya
hema ya kukutania, hapo nitakapokutana nawe; nayo yatakuwa kwenu matakatifu
sana. [37] Na uvumba utakaofanya, hamtajifanyia uvumba wenye viungo sawasawa na
uvumba huo; utakuwa kwenu mtakatifu kwa ajili yangu. [38] Mtu ye yote atakayefanya
mfano wa huo, ili kuunusa, mtu huyo atakatiliwa mbali na watu wake.

# 31

[1] Yahweh akasema na Musa, [2] "Angalia, nimemwita kwa jina lake Bezaleli mwana
wa Uri, mwana wa Huri, wa kabila ya Yuda [3] Nami nimemjaza Bezaleli na roho ya
Mungu, katika hekima, na maarifa, na ujuzi, na mambo ya kazi ya kila aina, [4] ili
abuni kazi za ustadi, kuwa fundi wa dhahabu, na wa fedha, na wa shaba, [5] na kukata
vito kwa kutiwa mahali, na kuchora miti, na kufanya kazi ya ustadi iwayo yote.
[6] Tena, nimemchagua, awe pamoja naye Oholiabu, mwana wa Ahisamaki, wa kabila
ya Dani. Nami nimetia hekima katika mioyo ya wote wenye moyo wa hekima, ili
wapate kufanya vyote nilivyokuagiza. Hii ni, [7] hema ya kukutania na sanduku la
ushuhuda, na kiti cha rehema kilicho juu yake, na vyombo vyote vya Hema; [8] na
meza, na vyombo vyake, na kinara cha taa safi pamoja na vyombo vyake vyote,
[9] na madhabahu ya kufukizia uvumba; na madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa na
vyombo vyake vyote, na birika na tako lake. [10] Pia mavazi yenye kufumwa kwa uzuri,
na mavazi matakatifu ya Haruni kuhani, na mavazi ya wanawe, ili kutumika katika
kazi ya ukuhani. [11] Pia mafuta ya kutiwa, na uvumba wa manukato mazuri, kwa ajili
ya mahali patakatifu; sawasawa na yote niliyokuagiza ndivyo watakavyofanya wao.

[12] akasema na Musa, [13] “Waambie wana wa Israeli, 'Hakika mtazishika Sabato zangu,
kwa kuwa ni ishara kati ya mimi na ninyi katika vizazi vyenu vyote; ili mpate kujua
ya kuwa mimi ndimi BWANA niwatakasaye ninyi. [14] Basi mtaishika hiyo Sabato; kwa
kuwa ni takatifu kwenu; kila mtu atakayeitia unajisi hakika yake atauawa; kwa kuwa
kila mtu afanyaye kazi katika siku hiyo, nafsi hiyo itakatiliwa mbali na watu wake.
[15] Kazi itafanywa siku sita; lakini siku ya saba ni Sabato ya kustarehe kabisa, takatifu
kwa BWANA; kila mtu atakayefanya kazi yo yote katika siku ya Sabato, hakika yake
atauawa. [16] Kwa ajili ya hayo wana wa Israeli wataishika Sabato. Kuiangalia sana
hiyo Sabato katika vizazi vyao vyote, ni agano la milele. [17] Ni ishara kati ya mimi
na wana wa Israeli milele; kwani kwa siku sita Yahweh alifanya mbingu na nchi,
akastarehe kwa siku ya saba na kupumzika. [18] Hapo Mungu alipokuwa amekwisha
zungumza na Musa katika mlima wa Sinai, akampa hizo mbao mbili za ushuhuda,
mbao mbili za mawe, zilizoandikwa kwa mkono wake.

# 32

[1] Hata watu walipoona ya kuwa Musa amekawia kushuka katika mlima, wakaku-
sanyana wakamwendea Aruni, wakamwambia, “Njoo, katufanyizie sanamu itakayok-
wenda mbele yetu, kwa maana Musa huyo aliyetutoa katika nchi ya Misri hatujui
yaliyompata.” [2] Hivyo Aruni akawaambia, “Zitoeni pete za dhahabu zilizo katika
masikio ya wake zenu, na wana wenu, na binti zenu, mkaniletee.” [3] Watu wote
wakavua pete za dhahabu zilizo katika masikio yao, na wakamletea Aruni. [4] Akapoke
mikononi mwao akaitengeneza kwa patasi, akaifanya iwe sanamu ya ndama kwa
kuiyeyusha. Nao wakasema, “Hiyo ndiyo miungu yako, Ee Israeli, iliyokutoa katika
nchi ya Misri.” [5] Naye Haruni alipoona jambo hili, akajenga madhabahu mbele yake;
Aruni akatangaza akasema, [6] “Kesho itakuwa sikukuu kwa Yahweh.” Wakaondoka
asubuhi na mapema, wakatoa dhabihu, wakaleta sadaka za amani, watu wakaketi
kula na kunywa, wakaondoka wacheze. [7] Kisha Yahweh akamwambia Musa, “Shuka
upesi, kwa maana watu wako uliowatoa katika nchi ya Misri wamejiharibu nafsi
zao. [8] Wamepotoka upesi kuiacha ile njia niliyowaamuru, wamejifanyizia ndama
ya kuyeyusha wakaiabudu na kuitolea dhabihu. Wakasema, 'Hiyo ndiyo miungu
yako, Ee Israeli, iliyokutoa katika nchi ya Misri. [9] Kisha Yahweh akamwambia
Musa, “Mimi nimewaona watu hawa, na tazama, ni watu wenye shingo ngumu.
[10] Basi sasa usinizuie. Ili hasira zangu ziwake juu yao, niwaangamize. Nami
nitakufanya wewe uwe taifa kuu.” [11] Musa akamsihi sana Yahweh Mungu wake, na
kusema,”Yahweh, kwa nini hasira zako kuwaka juu ya watu wako uliowaleta kutoka
nchi ya Misri kwa uweza mkuu, na kwa mkono wenye nguvu? [12] Kwa nini Wamisri
kusema, 'Amewatoa kwa kuwatenda uovu, ili apate kuwaua milimani, na kuwaondoa
watoke juu ya uso wa nchi?' Geuka katika hasira yako kali, ughairi uovu huu ulio
nao juu ya watu wako. [13] Mkumbuke Ibrahimu, na Isaka, na Israeli, watumishi
wako, ambao uliwaapia kwa nafsi yako, na kuwaambia, 'Nitazidisha kizazi chenu
mfano wa nyota za mbinguni; tena nchi hii yote niliyoinena nitakipa kizazi chenu
nao watairithi milele.'” [14] Na Yahweh akaughairi ule uovu aliosema ya kwamba
atawatenda watu wake. [15] Kisha Musa akageuka akashuka katika mlima, na zile mbao
mbili za mawe mikononi mwake. Mbao zilizoandikwa pande zote mbili, upande
huu na upande huu ziliandikwa. [16] Na zile mbao zilikuwa kazi ya Mungu nayo
maandiko yalikuwa maandiko ya Mungu, yaliyochorwa katika zile mbao. [17] Na
Yoshua aliposikia kelele za watu walipokuwa wakipiga kelele, akamwambia Musa,
“Kuna kelele ya vita kambini. [18] “Lakini Musa akasema, “Hiyo si sauti ya watu
wapigao kelele kwa sababu ya kushinda vitani, wala si sauti ya watu wapigao kelele
kwa sababu ya kushindwa; bali kelele za watu waimbao ndizo ninazozisikia mimi.”

[19] Hata alipoyakaribia kambini akaiona ile ndama, na watu wakicheza. Hasira ya
Musa ikawaka. Akazitupa zile mbao mikononi mwake, akazivunja chini ya mlima.
[20] Akaitwaa ile ndama waliyoifanya, akaichoma moto, akaisaga hata ikawa mavumbi,
akainyunyiza juu ya maji. Akawanywesha wana wa Israeli. [21] Musa akamwambia
Aruni, "Watu hawa wamekufanyani hata ukaleta dhambi hii kuu juu yao? [22] Aruni
akasema, "Hasira yako isiwake, bwana wangu. Wewe unawajua watu hawa, ya
kuwa wamejielekeza kwa mabaya. [23] Maana waliniambia, 'Katufanyie miungu,
itakayokwenda mbele yetu. Kwa maana mtu huyo Musa, aliyetutoa katika nchi
ya Misri, hatujui yaliyompata.' [24] Nikawaambia, 'Mtu ye yote aliye na dhahabu na
aivue; basi wakanipa, nami nikaitupa ndani ya moto, akatoka ndama huyu." [25] Basi
Musa alipoona ya kuwa watu hawa wameasi (maana Haruni amewaacha waasi, ili
wawe dhihaka kati ya adui zao) [26] Ndipo Musa akasimama katika mlango wa marago,
akasema, "Mtu awaye yote aliye upande wa Yahweh na aje kwangu." Wana wa Lawi
wote wakamkusanyikia. [27] Akawaambia, Yahweh, Mungu wa Israeli, asema hivi, 'Kila
mtu na ajifunge upanga wake pajani mwake, akapite huko na huko toka mlango hata
mlango kati ya marago, mkamchinje kila mtu ndugu yake, na kila mtu mwenziwe
na kila mtu jirani yake.'" [28] Na hao wana wa Lawi wakafanya kama vile alivyosema
Musa, wakaanguka siku ile kama watu elfu tatu. [29] Musa akasema, Jiwekeni wakfu
kwa Yahweh leo, kila mtu juu ya mwanawe na juu ya ndugu yake; ili Yahweh awape
baraka leo." [30] Hata asubuhi yake Musa akawaambia watu, "Mmetenda dhambi kuu.
Sasa nitakwenda juu kwa Yahweh. Labda nitafanya upatanisho kwa ajili ya dhambi
yenu." [31] Musa akarejea kwa Yahweh akasema," Oh! Watu hawa wametenda dhambi
kuu wamejifanyia miungu ya dhahabu. [32] Walakini sasa, ikiwa utawasamehe dhambi
yao – na kama sivyo, unifute, nakusihi, katika kitabu chako ulichoandika." [33] Yahweh
akamwambia Musa, "Mtu ye yote aliyenitenda dhambi ndiye nitakayemfuta katika
kitabu changu. [34] Basi sasa uende ukawaongoze watu hawa mpaka mahali pale
ambapo nimekwambia habari zake. Tazama, malaika wangu atakutangulia. Lakini
pamoja na hayo siku nitakayowajilia nitawapatiliza kwa ajili ya dhambi yao." [35] Kisha
Yahweh akawapiga hao watu, kwa walivyoifanya ile ndama, ambayo Aruni aliifanya.

# 33

[1] Yahweh anasema na Musa, "Nenda kutoka hapa, wewe na watu ulio watoa
kutoka nchi ya Misri. Nenda kwenye nchi nilio fanya nadhiri na Ibrahimu, Isaka,
Yakobo, nilipo sema, 'Nitakupa wewe na uzao wako'.' [2] Nitatuma malaika mbele
yako, na kuwaondoa Wakanani, Waamori, Wahiti, Waperizi, Wahivi, na Wayebusi.
[3] Nenda kwenye hiyo nchi, inayo tiririka kwa maziwa na asali, lakini sitaenda nawe,
kwasababu ninyi ni watu wajehuri. Ninaweza kuwaharibu njiani." [4] Watu walipo
sikia haya maneno ya kushtua, walilia, na hakuna aliye vaa mikufu. [5] Yahweh
alisema kwa Musa, "Waambie Waisraeli, 'Ninyi ni watu wakorofi. Kama ningeenda
miongoni mwenu ata kwa muda kidogo, nigewaharibu ninyi. Hivyo sasa, toa mikufu
yenu ili niamue nini cha kufanya kwenu."' [6] Hivyo Waisraeli hawaku vaa mikufu
kutoka Mlima Horebu na kwendelea. [7] Musa akachukua hema na kukita nje ya
kambi, umbali kidogo na kambini. Aliita hema ya kukutania. Kila mtu alliye
muuliza Yahweh kitu chochote alienda kwenye hema ya kukutania, nje ya kambi.
[8] Kisha Musa alipo enda kwenye hema, watu wote walisima kando ya hema yao
na kumuangalia Musa hadi alipo ingia ndani. [9] Wakati wowote Musa alipo ingia
hemani, nguzo ya wingu ilishuka chini na kusimama nje ya lango la hema, na
Yahweh alizungumza na Musa. [10] Wakati wowote watu walipo ona nguzo ya wingu
imesimama langoni mwa hema, waliamka na kuabudu, kila langoni mwa hema
yake. [11] Yahweh alizungumza na Musa uso kwa uso, kama mtu anapo zungumza

na rafiki yake. Kisha Musa alirudi kambini, lakini mtumishi wake Yoshua mwana wa
Nuni, kijana, alibaki hemani. 12 Musa alisema na Yahweh, “Ona, umekuwa ukisema
na mimi, 'Chukuwa watu hawa safarini,' lakini hauja niambia nani utamtuma na
mimi. Umesema, 'Nina kujua kwa jina, na umepata upendeleo kwangu.' 13 Kama
nimepata upendeleo machoni pako, nionyeshe njia zako ili nikujue na kuendelea
kupata upendeleo machoni pako. Kumbuka ili taifa ni watu wako.” 14 Yahweh
akajibu, “Uwepo wangu utaenda nawe, na nitakupa pumziko.” 15 Musa akasema,
“Kama uwepo wako hautaenda nasi, usitutoe hapa. 16 Au je, itajulikanaje niimepata
upendeleo machoni pako, mimi na watu wako? Haitakuwa kuwa tu kama ukienda
nasi mimi na watu wako tutakuwa na utofauti na watu wengine wote waliopo katika
uso wa dunia?” 17 Yahweh akamwambia Musa, “Nitafanya pia hichi kitu ulicho
niomba, kwa kuwa umepata upendeleo machoni mwangu, na nina kujua kwa jina
lako.” 18 Musa akasema, Tafadhali nionyeshe utukufu wako.” 19 Yahweh akasema,
“Nitafanya wema wangu wote ujulikani kwako, na nitatangaza jina langu 'Yahweh'
kwako. Nitakuwa na neema kwake nitakae kuwa na neema, na nitaonyesha rehema
kwake nitakaye onyesha rehema.” 20 Lakini Yahweh akasema, “Hauta ona uso wangu,
kwa kuwa hakuna aonaye uso wangu na kuiishi.” 21 Yahweh akasema, “Ona, hapa
kuna sehemu yangu; utasimama kwenye huu mwamba. 22 Wakati utukufu wangu
unapita, nitakuweka kwenye shimo kubwa la mwamba na kukufunika kwa mkono
wangu mpaka nitakapo pita. 23 Kisha nitaondoa mkono wangu, na utaona mgongo
wangu, ila uso wangu hautaonekana.”

# 34

1 Yahweh akamwabia Musa, “Kata mbao mbili za mawe kama zile za awali.
Nitaandika kwenye hizi mbao za mawe maneno yaliyo kuwa kwenye mbao za mawe
za mwanzo, mbao za mawe ulizo zivunja. 2 Kuwa tayari asubui na uje Mlima Sinai, na
uje mbele zangu juu ya mlima. 3 Hakuna atakaye kuja nawe. Usiruhusu mtu yeyote
aonekana popote kwenye mlima. Hakuna kundi la mifugo wanao ruhusiwa ata kula
mbele ya mlima.” 4 Hivyo Musa akakata mbao mbili za mawe kama za mwanzo,
na akaamka asubui mapema na kwenda juu ya Mlima Sinai, kama Yahweh alivyo
muelekeza. Musa alibeba mbao za mawe mikononi mwake. 5 Yahweh akaja chini
katika wingu na akasima mbele za Musa, na akatamka jina “Yahweh.” 6 Yahweh
akapita kwake na kukiri, “Yahweh, Yahweh, Mungu ni wa rehema na wa neema, sio
mwepesi wa hasira, na anadumu katika uwaminifu wa agano na uadilifu, 7 ukishika
uaminifu wa agano kwa vizazi maelfu, ukisamehe maasi, makosa, na dhambi. Lakini
hamsafishi mwenye hatia. Ataleta adhabu ya dhambi za baba kwa watoto wao
na watoto wa watoto wao, kwa kizazi cha tatu na hadi cha nne.” 8 Musa haraka
akainamisha kichwa chake kwenye ardhi na kuabudu. 9 Kisha akasema, “Kama sasa
nimepata upendeleo machoni pako, Bwana wangu, tafadhali nenda pamoja nasi, kwa
kuwa hawa watu ni wa korofi. Samehe maasi yetu na dhambi zetu, na utuchukuwe
kama urithi wako.” 10 Yahweh akasema, “Ona, ninakaribu kufanya agano. Mbele
za watu wako, nitafanya maajabu ambayo hayajawai kufanywa duniani kote wala
kwenye taifa lote. Watu wote miongoni mwako wataona matendo yangu, kwa kuwa
ni kitu cha hofu ninacho fanya kwako. 11 Tii amri zangu leo. Ninawaondoa mbele
yako Waamori, Wakanani, Wahivi, Wahiti, Waperizi, Wahivi, na Wayebusi. 12 Kuwa
mwanglifu usifanye agano na wakazi wa nchi unayo kwenda, au wata kuwa mtego
kwako. 13 Badala yake, lazima uvunje madhabahu zao, ponda nguzo zao za mawe,
na kukata nguzo zao za Ashera. 14 Kwa kuwa wewe haupaswi kumuabudu mungu
mwingine, maana Yahweh, ambaye jina lake ni Uwivu, ni Mungu wa uwivu. 15 Hivyo
kuwa mwangalifu usifanye agano na wakazi wa nchi, kwa kuwa wanajifanyia

ukahaba kwa miungu yao, na wanatoa dhabihu kwa miungu yao. Kisha mmoja wao
ata kukaribisha na wewe utakula baadhi ya dhabihu zake, 16 na kisha utachukuwa
baadhi ya mabinti zake kwa wanao, na mabinti wake watafanya ukahaba kwa
miungu yao, na watafanya wanao kufanya ukahaba kwa miungu yao. 17 Usifanye
Miungu ya chuma ya kuyayusha. 18 Laziam ushike Sherehe ya Mkate Usiotiwachachu.
Kama nilivyo kuamuru, lazima ule mkate usio na hamira kwa siku saba kwa muda
uliotengwa wa mwezi wa Abibu, maana nikatika mwezi wa Abibu ulitoka Misri.
19 Wazaliwa wote ni mwangu, ata mzaliwa wa kwanza wa kiume wa mifugo, yote
ya ng'ombe na kondoo. 20 Lazima umnunue tena mzaliwa kwanza wa punda kwa
kondoo, lakini usipo mnunua tena, kisha uivunje shingo yake. Lazima ununue tena
wazaliwa wa kwanza wote wa wanao. Hakuna ata mmoja atakye kuja kwangu
mikono mitupu. 21 Utafanya kazi kwa siku sita, lakini siku ya saba utapumzika. Ata
wakati wakilimo na wa mavuno, lazima upumzike. 22 Lazima uadhimishe Sherehe
ya Majuma kwa mazao ya kwanza ya mavuno ya ngano, na lazima uadhimishe
Sherehe ya Makusanyo mwisho wa mwaka. 23 Mara tatu kwa mwaka wanaume wenu
wote watajitokeza kwa Bwana Yahweh, Mungu wa Israeli. 24 Kwa kuwa nitaondoa
mataifa mbele yenu na kutanua mipika. Hakuna atakaye tamani kuwa na ardhi
yenu kama yao utakapo toka mbele za Yahweh mara tatu kwa mwaka. 25 Hautatoa
damu ya dhabihu yangu na hamira yeyote, wala nyama yeyote kutoka dhabihu za
Sherehe ya Pasaka kubaki hadi asubui. 26 Lazima ulete matunda ya kwanza yalio bora
kutoka nyumbani kwako. Usimchemshe mbuzi mtoto katika maziwa ya mama yake."
27 Yahweh akamwabia Musa, "Andika chini haya maneno, kwa kuwa nimejiahidi
haya maneno niliyo yasema, na nimefanya agano kwako na Israeli." 28 Musa alikuwa
huko na Yahweh kwa siku arobaini na usiku; hakula chakula chochote wala kunywa
maji yeyote. Aliandika katika mbao maneno ya agano, Amri kumi. 29 Musa alipo
shuka chini ya Mlima Sinai na mbao mbili za agano za ushuhuda mikononi mwake,
hakujua kuwa ngozi ya kuwa uso wake ulikuwa wa'ngaa akizungumza na Mungu.
30 Wakati Aruni na Waisraeli walipo muona Musa, ngozi ya uso wake ulikuwa wa
ng'aa, na waliogopa kuja karibu yake. 31 Lakini Musa aliwaita, na Aruni na viongozi
wa jamii wakaja kwake. Kisha Musa akasema nao. 32 Baada ya haya, watu wote wa
Israeli wakaja kwa Musa, na akawambia amri zote Yahweh alizo mpa katika Mlima
Sinai. 33 Musa alipo maliza kuzungumza nao, alifunika uso wake kwa kitambaa.
34 Wakati Musa alipoenda mbele za Yahweh kusema naye, aliondoa kitambaa, hadi
alipo toka. Alipo toka, aliwaambia Waisraeli alicho amriwa kusema. 35 Waisraeli
walipo muona Musa ana'ngaa uso, alirudisha kitambaa tena usoni mpaka alipokuwa
anaenda kuongea na Yahweh.

# 35

1 Musa akawakusanya jamii yote ya Waisraeli na kuwaambia, "Haya ndio mambo
Yahweh aliyo waamuru mfanye. 2 Kwa siku sita kazi ya weza fanywa, lakini kwako,
siku ya saba lazima iwe siku takatifu, siku ya Sabato ya mapumziko, takatifu kwa
Yahweh. Yeyote atakaye fanya kazi hiyo siku lazima auawe. 3 Haupaswi kuwasha
moto kwenye nyumba zenu siku ya Sabato." 4 Musa akasema na jamii yote ya
Waisraeli, kwa kusema, "Hichi ndicho kitu Yahweh alicho amuru. 5 Chukuwa sadaka
kwa ajili ya Yahweh, wote wenye moyo mkunjufu. Leta sadaka kwa Yahweh -
dhahabu, fedha, shaba, 6 buluu, zambarau, sufu nyekundu na kitambaa kizuri;
nywele za mbuzi; 7 ngozi za kondoo zilizotiwa rangi nyekundu na ngozi za pomboo;
na mbao za mshita; 8 mafuta ya taa kwa pahali patakatifu, viungo vya manukato
kwa hayo mafuta ya kutiwa, 9 kwa uvumba mzuri na vito vya shohamu na vito
vya kutiwa kwa hiyo naivera, na kwa hicho kifuko cha kifuani. 10 Kila mwanaume

mwenye ustadi kati yenu aje na afanye kila kitu ambacho Yahweh aliyaamuru —
[11] hema la kuabudia, na kifuniko chake, na vifungo vyake, na mbao zake, nguzo, na
sakafu; [12] pia sanduku na nguzo zake, kiti cha rehema, na pazia la kusitiri. [13] Walileta
meza na miguu yake, vyombo vyake vyote, na mkate wa wonyesho; [14] kinara cha taa,
vyombo vyake, taa, na mafuta ya zile taa; [15] ile madhabahu ya uvumba na nguzo zake,
mafuta ya upako na uvumba ulitiwa maukato; kishikizo cha mwingilio wa hema ya
kuabudia; [16] madhabahu ya sadaka ya kuteketeza na kitunzi cha shaba na nguzo
na vyombo; na ile beseni kubwa na sakafu yake. [17] Walileta vishikizo kwa ajili ya
nyuani na nguzo zake na sakafu yake, na pazia kwa ajili mwingilio wa nyauni; [18] na ile
misumari ya hema la kuabudia na nyuani, pamoja na kamba zake. [19] Walileta mavazi
yaliyofumwa kutumikia sehemu takatifu, mavazi takatifu ya Aruni kuhani na wanae,
kwa wao kutumika kama makuhani." [20] Kisha makabila yote ya Israeli yakaondoka
na kwenda kutoka uweponi mwa Musa. [21] Kila mtu moyo wake ulimchochea na
aliye andaliwa na roho yake alikuja na kuleta sadaka kwa Yahweh kwa matengenezo
ya hema ya kuabudia, kwa vitu vyote kwajili ya huduma ndani yake, na kwa vazi
takatifu. [22] Walikuja, wote wanaume kwa wanawake, wote waliokuwa na moyo wa
utayari. Walileta madini, hereni, pete, na vitu vya thamani, vitu vyote tofauti vyenye
madini ya dhahabu. Waliwasilisha sadaka za dhahabu kama sadaka ya kupunga kwa
Yahweh. [23] Kila mmoja alikuwa na sufu ya buluu, dhambarau, au nyekundu, nguo
nzuri, singa za mbuzi, ngozi za kondoo zilizobadili kuwa nyekundu, na ngozi ya
pomboo walivileta. [24] kila mmoja alitengeneza sadaka ya fedha au shaba walizileta
kama sadaka kwa Yahweh, na kila mmoja aliyekuwa na mti wa mshita kwa matumizi
ya kazi aliuleta. [25] kila mwanamke mwenye ustadi walisokota sufu kwa mikono yao
na walileta sufu walizosokota za buluu, dhambarau, au sufu nyekundu, au nguo
nzuri. [26] Wanawake wote wenye mioyo iliyochochewa na walio na ustadi walisokota
singa za mbuzi. [27] Viongozi walileta mawe ya shohamu na mawe mengine kwaajili
ya kuwekwa kwenye hiyo naivera na hicho kifuko cha kifuani; [28] walileta viungo
na mafuta kwaajili ya taa, kwa mafuta ya upako, na kwa uvumba wa manukato.
[29] Waisraeli walileta sadaka ya hiyari kwa Yahweh; kila mwanaume na mwanamke
ambao mioyo yao ilikuwa tayari walileta vifaa kwaajili kazi zote ambazo Yahweh
aliamuru kupitia Musa zifanyike. [30] Musa alisema kwa waisraeli, "Tazama, Yahweh
ameita kwa jina juu ya Bezaleli mwana wa Uri mwana wa Huri, kutoka kabila la
Yuda. [31] Aliijaza Bezaleli kwa Roho yake, kumpa hekima, uwelewa, na maarifa,
kwa aina zote za ujenzi, [32] kufanya sanaa ya ubunifu na kufanya kazi za dhahabu,
shaba, na shaba; [33] pia kukata na kupanga mawe na mbao iliochongwa- kufanya kazi
za aina zote kwa ubunifu na ujenzi. [34] Aliiweka kufundisha ndani ya moyo wake,
yeye pamoja na Oholiabu mwana wa Ahisamaki, kutoka kabila la Dani. [35] Aliwajaza
kwa ustadi wa kufanya kazi za aina zote, kufanya kazi ya kama kuchora mawe,
kama mwerevu, kama mtia taraza katika nyuzi za rangu ya buluu, dhambarau, na
nyekundu na nguo nzuri, na kama washonaji. Walikuwa wachonga mawe wa kazi
zote, na walikuwa wabunifu wa sanaa.

## 36

[1] Hivyo Bezaleli na Oholiabu na kila mtu mwenye ustadi ambaye Yahweh aliye
mpa ustadi na uwezo kujua jinsi ya kufanya kazi katika ujenzi wa sehemu takatifu
wafanye kazi kadiri ya yote Yahweh aliyo amuru." [2] Musa akamuita Bezaleli,
Oholiabu, na kila mtu mwenye ujuzi ambaye Yahweh kampa ujuzi, na ambaye
moyoni mwake ulichochewa kuja na kufanya kazi. [3] Walipokea kutoka kwa Musa
sadaka zote ambazo Waisraeli walizo leta kwa ujenzi ya sehemu takatifu. Watu
walikuwa bado wanaleta sadaka za hiari kila asubui kwa Musa. [4] Hivyo watu

wote walikuwa na ujuzi walikuwa wakifanya kazi sehemu takatifu walikuja kutoka
kwenye kazi walikuwa wakifanya. 5 Wachonga mawe walimwabia Musa, "Watu
wanaleta zaidi sana ya yanayo itajika kufanya kazi Yahweh aliyo tuamuru." 6 Hivyo
Musa akaamuru mtu yeyote asilete tena kwa ujenzi wa sehemu takatifu. Kisha
watu wakaacha kuleta hivi vitu. 7 Walikuwa na zaidi ya vitu vya ujenzi. 8 Hivyo
wachonga mawe miongoni mwao wakajenga lile hema la kuabudia kwa mapazia
kumi yaliyo jengwa kitamba kizuri na buluu, zambarau, na sufu nyekundu kwa
aina ya kerubi. Hii ni kazi ya Bezaleli, mjenzi mwenye ujuzi sana. 9 Urefu wa kila
pazia ulikuwa mikono ishirini na nane, nao upana wa kila kitambaa ulikuwa mikono
minne. Vitambaa vyote hivyo vilikuwa na kipimo kimoja. 10 Bezaleli akaunganisha
vitambaa vitano pamoja, na vile vitambaa vingine vitano akaviunganisha pamoja.
11 Kisha akafanya vitanzi vya uzi wa bluu kwenye upindo wa kitambaa kilicho
mahali pa kuungania. Akafanya vivyo hivyo kwenye upindo wa kitambaa cha nje
kabisa kilicho mahali pale pengine pa kuungania. 12 Akafanya vitanzi hamsini
kwenye kitambaa kimoja, akafanya vitanzi hamsini kwenye mwisho wa kitambaa
kilichokuwa mahali pale pengine pa kuungania, vitanzi hivyo vikiwa vinaelekeana.
13 Mwishowe akafanya kulabu hamsini za dhahabu na kuviunganisha vitambaa
hivyo pamoja kwa kulabu hizo, hivi kwamba hiyo ikawa maskani moja. 14 Bezaleli
akafanya vitambaa vya mahema vya manyoya ya mbuzi kwa ajili ya hema lililo juu ya
maskani. Vitambaa kumi na moja ndivyo alivyofanyiza. 15 Urefu wa kila kitambaa
ulikuwa mikono thelathini, nao upana wa kila kitambaa ulikuwa mikono minne.
Vitambaa hivyo kumi na moja vilikuwa na kipimo kimoja. 16 Kisha akaunganisha
vitambaa vitano pamoja na vile vitambaa vingine sita pamoja. 17 Kisha akafanya
vitanzi hamsini kwenye upindo wa kitambaa cha nje kabisa kilicho mahali pa
kuungania, naye akafanya vitanzi hamsini kwenye upindo wa kile kitambaa kingine
kilichoungana nacho. 18 Bezaleli akafanya kulabu hamsini za shaba kwa ajili ya
kuliunganisha hilo hema pamoja liwe kipande kimoja. 19 Naye akafanya kifuniko
cha hema kutokana na ngozi za kondoo dume zilizotiwa rangi nyekundu na kifuniko
kutokana na ngozi za sili, upande wa juu. 20 Bezaleli akafanya viunzi vya mbao
vya hema ya kukutani kutokana na mbao za mshita. 21 Urefu wa kiunzi ulikuwa
mikono kumi, nao upana wa kila kiunzi ulikuwa mkono mmoja na nusu. 22 Kila
kiunzi kilikuwa na ndimi mbili zilizounganishwa. Hivyo ndivyo alivyofanya viunzi
vyote vya maskani. 23 Basi akafanya viunzi vya maskani, viunzi ishirini kwa ajili
ya upande kuelekea kusini. 24 Bezaleli akafanya vikalio arobaini vya fedha viwe
chini ya vile viunzi ishirini, vikalio viwili chini ya kiunzi kimoja pamoja na ndimi
zake mbili na vikalio vingine viwili chini ya kiunzi kingine pamoja na ndimi zake
mbili. 25 Na kwa ajili ya ule upande mwingine wa maskani, upande wa kaskazini,
akafanya viunzi ishirini 26 na vikalio vyake arobaini vya fedha. Vikalio viwili chini ya
kiunzi kimoja na vikalio viwili chini ya kiunzi kingine 27 Na kwa ajili ya zile pande
za nyuma za maskani kuelekea magharibi akafanya viunzi sita. 28 Naye akafanya
viunzi viwili vya pembeni ya maskani kwenye pande zake mbili za nyuma 29 Hizi
zilikuwa pacha upande wa chini, lakini juu ya kila moja kwenye pete ya kwanza.
Hivyo ndivyo alivyoifanya yote miwili, ile miimo ya pembeni. 30 Basi vikajumlika
kuwa viunzi vinane na vikalio vyake kumi na sita vya fedha, vikalio viwili kando
ya vikalio viwili chini ya kila kiunzi. 31 Bezaleli akafanya miti ya mshita, mitano
kwa ajili ya viunzi vya upande mmoja wa maskani, 32 na miti mitano kwa ajili ya
viunzi vya upande ule mwingine wa maskani na miti mitano kwa ajili ya viunzi vya
maskani kwa ajili ya zile pande mbili za nyuma za magharibi. 33 Kisha akafanya mti
wa katikati upitie katikati ya vile viunzi toka mwisho mmoja mpaka ule mwingine.
34 Naye akavifunika vile viunzi kwa dhahabu, akafanyiza pete zake za dhahabu ziwe

vitegemezo kwa ajili ya ile miti, akaifunika ile miti kwa dhahabu. 35 Bezaleli akafanya
pazia, la uzi wa bluu na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa cha rangi
nyekundu ya kochinili na kitani bora kilichosokotwa, kalitia makerubi kwa kazi ya
mjenzi. 36 Kisha akalifanyia nguzo nne za mshita na kuzifunika kwa dhahabu, vibanio
vyake vikiwa vya dhahabu, na kutengeneza vikalio vinne vya fedha kwa ajili yake.
37 Naye akafanya kisitiri kwa ajili ya mwingilio wa hema kutokana na uzi wa bluu na
sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili na
kitani bora kilichosokotwa, kazi ya mfumaji. 38 Pia akafanya na nguzo zake tano na
vibanio vyake. Naye akavifunika vilele vyake na viungo vyake kwa dhahabu, lakini
vile vikalio vyake vitano vilikuwa vya shaba.

# 37

1 Bezaleli akafanya Sanduku la mbao za mshita. Mikono miwili na nusu urefu
wake, na mkono mmoja na nusu upana wake, na mkono mmoja na nusu kimo chake.
2 Kisha akalifunika kwa dhahabu safi ndani na nje na kulifanyia ukingo wa dhahabu
kulizunguka pande zote. 3 Kisha akalitengenezea pete nne za dhahabu, za juu ya
miguu yake minne, pete mbili upande wake mmoja na pete mbili upande wake
mwingine 4 Kisha akafanya miti ya mshita na kuifunika kwa dhahabu. 5 Halafu
akaitia miti hiyo kwenye zile pete zilizo pande za Sanduku ili kulibeba Sanduku.
6 Naye akafanya kifuniko cha dhahabu safi. Mikono miwili na nusu urefu wake,
na mkono mmoja na nusu upana wake. 7 Bezaleli akafanya makerubi wawili wa
dhahabu. Kwa kazi ya kufua akawafanya kwenye miisho yote miwili ya kifuniko.
8 Kerubi mmoja kwenye mwisho ule, na yule kerubi mwingine kwenye mwisho huu.
Aliwafanya makerubi juu ya kifuniko kwenye miisho yote miwili. 9 Nao wakawa
makerubi wanaonyoosha mabawa yao mawili kuelekea juu, wakisitiri kifuniko
kwa mabawa yao, nazo nyuso zao zilikuwa zikielekeana. Nyuso za makerubi hao
zilielekea kifuniko hicho. 10 Bezaleli akafanya meza ya mbao za mshita. Mikono
miwili urefu wake, na mkono mmoja upana wake, na mkono mmoja na nusu kimo
chake. 11 Halafu akaifunika kwa dhahabu safi na kufanya ukingo wa dhahabu
kuizunguka pande zote. 12 Kisha akafanya mzingo wa upana wa kiganja kuizunguka
na kufanya ukingo wa dhahabu kwa ajili ya mzingo wake kuizunguka pande zote.
13 Tena, akatengeneza pete nne za dhahabu kwa ajili yake na kuziweka pete hizo
kwenye zile pembe nne zilizokuwa kwa ajili ya ile miguu minne. 14 Pete hizo zilikuwa
karibu na ule mzingo, ili kutegemeza ile miti ya kuibeba meza hiyo. 15 Halafu
akafanya ile miti ya mshita na kuifunika kwa dhahabu ili kuibeba ile meza. 16 Baada
ya hilo akafanya kutokana na dhahabu safi vile vyombo vilivyo juu ya meza, sahani
zake na vikombe vyake na mabakuli yake na mitungi yake iliyotumiwa kumimina
matoleo ya kinywaji. 17 Kisha akafanya kinara cha taa cha dhahabu safi. Kwa kazi
ya kufua akakifanya kinara cha taa. Pande zake na matawi yake, vikombe vyake,
mafundo yake na maua yake vikatokea kwake. 18 Na matawi sita yalikuwa yakitoka
kwenye pande zake, matawi matatu ya kinara cha taa kutoka kwenye upande wake
mmoja na matawi mengine matatu ya kinara cha taa kutoka kwenye ule upande
wake mwingine. 19 Vikombe vitatu vyenye umbo la maua ya mlozi vilikuwa kwenye
kikundi kimoja cha matawi, vifundo na maua yakifuatana; na vikombe vitatu vyenye
umbo la maua ya mlozi vilikuwa kwenye kile kikundi kingine cha matawi, vifundo
na maua yakifuatana. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa yale matawi sita yaliyokuwa
yakitoka katika kile kinara cha taa. 20 Na kwenye kile kinara cha taa kulikuwa
na vikombe vinne vyenye umbo la maua ya mlozi, vifundo vyake na maua yake
yakifuatana. 21 Na kile kifundo chini ya matawi mawili kilitoka kwake, na kifundo
kilicho chini ya yale matawi mengine mawili kilitoka kwake, na kifundo kingine

kilicho chini ya matawi mengine mawili zaidi kilitoka kwake, kwa ajili ya matawi
sita yanayotoka katika kinara. 22 Vifundo vyake na matawi yake vilitoka kwake,
vyote vilikuwa kitu kimoja cha kazi ya kufua, cha dhahabu safi. 23 Kisha akafanya
taa zake saba na mikasi ya tambi zake na vyetezo vyake kutokana na dhahabu safi.
24 Alikifanya kwa talanta ya dhahabu safi, hicho pamoja na vyombo vyake vyote.
25 Sasa akafanya madhabahu ya uvumba+ kutokana na mbao za mshita. + Mkono
mmoja urefu wake na mkono mmoja upana wake, ikiwa mraba, na mikono miwili
kimo chake. Pembe zake zilitoka kwake. 26 Kisha akaifunika kwa dhahabu safi,
upande wake wa juu na pande zake za kando kuizunguka na pembe zake, naye
akafanya ukingo wa dhahabu kuizunguka pande zote. 27 Naye akaifanyia pete mbili
za dhahabu chini ya ukingo wake kwenye pande zake mbili, kwenye pande zake
mbili zinazoelekeana, za kutegemeza ile miti ya kuibeba. 28 Kisha akafanya ile miti ya
mshita na kuifunika kwa dhahabu. 29 Tena akafanya yale mafuta yanayotumiwa kutia
mafuta na ule uvumba safi uliotiwa manukato, + kazi ya mtengenezaji wa marhamu.

# 38

1 Naye akafanya madhabahu ya toleo la kuteketezwa kwa mbao za mshita. Mikono
mitano urefu wake, na mikono mitano upana wake, ilikuwa mraba, na mikono mitatu
kimo chake. 2 Halafu akafanya pembe zake kwenye zile ncha zake nne. Pembe zake
zilitoka kwake. Kisha akaifunika kwa shaba. 3 Baada ya hilo akavifanya vyombo
vyote vya madhabahu, yale makopo na zile sepetu na yale mabakuli, zile nyuma
na vile vyetezo. Vyombo vyake vyote alivifanya kwa shaba. 4 Tena akaifanyia
madhabahu kiunzi cha fito, mtandao wa shaba, chini ya ukingo wake, chini kuelekea
katikati yake. 5 Halafu akatengeneza pete nne kwenye ile miisho minne karibu na
kile kiunzi cha shaba, ili kuitegemeza ile miti. 6 Bezaleli akafanya miti ya mshita
na kuifunika kwa shaba. 7 Kisha akaitia ile miti kwenye zile pete zilizo pande za
madhabahu ili kuibeba. Akaifanya kuwa sanduku la mbao lenye uwazi. 8 Kisha
akafanya beseni ya shaba na kinara chake cha shaba. Kwa kutumia vioo vya
watumishi wanawake ambao walifanya utumishi uliopangwa kwenye mwingilio wa
hema la mkutano. 9 Naye akafanya ule ua. Upande unaokabili Negebu, kuelekea
kusini, mapazia ya ua yalikuwa ya kitani bora kilichosokotwa, kwa mikono mia moja.
10 Nguzo zake ishirini na vikalio vyake ishirini vilikuwa vya shaba. Misumari ya
nguzo na viungo vyake vilikuwa vya fedha 11 Pia, kwa ajili ya upande wa kaskazini
kulikuwa na mikono mia. Nguzo zake ishirini na vikalio vyake ishirini vilikuwa vya
shaba. Misumari ya nguzo na viungo vyake vilikuwa vya fedha. 12 Lakini kwa ajili
ya upande wa magharibi mapazia yalikuwa mikono hamsini. Nguzo zake zilikuwa
kumi na vikalio vyake kumi. Misumari ya nguzo na viungo vyake vilikuwa vya fedha.
13 Na kwa ajili ya upande wa mashariki kulikuwa na mikono hamsini. 14 Mapazia
yalikuwa mikono kumi na mitano kwa upande mmoja. Nguzo zake zilikuwa tatu
na vikalio vyake vitatu. 15 Na kwa ajili ya upande ule mwingine, huu na ule, wa
lango la ua, mapazia yalikuwa mikono kumi na mitano. Nguzo zake zilikuwa tatu na
vikalio vyake vitatu. 16 Mapazia yote ya ua kuzunguka pande zote yalikuwa ya kitani
bora kilichosokotwa. 17 Navyo vikalio vya nguzo vilikuwa vya shaba. Vibanio vya
vikalio na viungo vyake vilikuwa vya fedha navyo vilifunikwa kwa shaba sehemu
ya juu, na kulikuwa na viungo vya shaba kwa ajili ya nguzo zote za ua. 18 Nacho
kisitiri cha lango la ua kilikuwa na mikono ishirini urefu. Cha uzi wa bluu na
sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili
na kitani bora kilichosokotwa, na urefu wake ulikuwa mikono ishirini, nacho kimo
kotekote kilikuwa mikono mitano sawasawa na mapazia ya ua. 19 Na nguzo zake
nne na vikalio vyake vinne vilikuwa vya shaba. Misumari yake ilikuwa ya fedha

na utando wa vichwa vyake na viungo vyake ulikuwa wa fedha. [20] Na misumari
yote ya hema kwa ajili ya maskani na kwa ajili ya ua kuzunguka pande zote ilikuwa
ya shaba [21] Hivi ndivyo vitu vilivyohesabiwa vya maskani, maskani ya Ushuhuda,
vilivyohesabiwa kwa amri ya Musa, kuwa utumishi wa Walawi chini ya uongozi wa
Ithamari mwana wa Aruni kuhani. [22] Naye Bezaleli mwana wa Uri mwana wa Huru
wa kabila la Yuda alifanya yote ambayo Yahweh alikuwa amemwamuru Musa. [23] Na
pamoja naye alikuwa Oholiabu mwana wa Ahisamaki wa kabila la Dani, fundi na
mtarizi na mfumaji wa uzi wa bluu na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa
chenye rangi nyekundu ya kochinili na kitani bora. [24] Dhahabu yote iliyotumiwa kwa
ajili ya kazi katika kazi yote ya mahali patakatifu ikawa jumla ya dhahabu ya toleo
la kutikisa, + talanta ishirini na tisa na shekeli 730 kulingana na shekeli+ ya mahali
patakatifu. [25] Nayo fedha ya wale walioandikishwa kati ya kusanyiko ilikuwa talanta
mia moja na shekeli 1, 775 kulingana na shekeli ya mahali patakatifu, [26] ile nusu
shekeli kwa ajili ya mtu mmoja ilikuwa nusu shekeli kulingana na shekeli ya mahali
patakatifu,. Kwa kila mtu aliyekuwa akipita kuingia upande wa wale waliokuwa
wameandikishwa kuanzia miaka ishirini na zaidi, jumla ya watu 603, 550. [27] Na
talanta mia moja za fedha zilitumiwa kutengeneza vikalio vya mahali patakatifu na
vikalio vya lile pazia. Vikalio mia moja vilitoshana na talanta mia moja, talanta
moja kwa kikalio kimoja. [28] Na kutokana na zile shekeli 1, 775 alifanyiza vibanio vya
nguzo na kuvifunika sehemu yake ya juu na kuviunganisha pamoja. [29] Nayo shaba ya
toleo la kutikisa ilikuwa talanta sabini na shekeli 2, 400. [30] Naye akaitumia kufanya
vile vikalio vya mwingilio wa hema la mkutano na ile madhabahu ya shaba na kile
kiunzi chake cha shaba, na vyombo vyote vya madhabahu, [31] na vile vikalio vya ua
kuzunguka pande zote, na vile vikalio vya lango la ua, na misumari yote ya maskani
na misumari+ yote ya ua kuzunguka pande zote.

# 39

[1] Na kutokana na ule uzi wa bluu na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na
kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili wakafanya mavazi yaliyofumwa kwa
ajili ya kuhudumu katika mahali patakatifu. Basi wakafanya yale mavazi matakatifu
yaliyokuwa kwa ajili ya Aruni, kama vile Yahweh alivyokuwa amemwamuru Musa.
[2] Basi akaifanya ile naivera ya dhahabu, uzi wa bluu na sufu iliyotiwa rangi
ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili na kitani bora
kilichosokotwa. [3] Kisha wakafua mabamba ya dhahabu yawe mabamba membamba,
naye akakata nyuzi za kufuma pamoja na ule uzi wa bluu na ile sufu iliyotiwa rangi
ya zambarau na kile kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili na kile kitani
bora, kama kazi ya mjenzi. [4] Wakaifanyia vipande vya begani vilivyounganishwa.
Iliunganishwa kwenye miisho yake miwili. [5] Nao mshipi, uliokuwa juu yake ili
kuifunga, ulikuwa wa kitambaa kilekile kulingana na ufundi wake, wa dhahabu, uzi
wa bluu, na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya
kochinili na kitani bora kilichosokotwa, kama vile Yahweh alivyokuwa amemwamuru
Musa. [6] Kisha wakafanya mawe ya shohamu yaliyopangwa kwenye mapambo ya
dhahabu, yaliyochongwa kwa michoro ya muhuri kulingana na majina ya wana wa
Israeli. [7] Bezaleli akayaweka kwenye vile vipande vya begani vya naivera yawe
mawe ya ukumbusho kwa ajili ya wana wa Israeli, kama vile Yehova alivyokuwa
amemwamuru Musa. [8] Kisha akafanya kile kifuko cha kifuani kwa ufundi wa mjenzi,
kama ule ufundi wa naivera, kutokana na dhahabu, uzi wa bluu na sufu iliyotiwa
rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili na kitani bora
kilichosokotwa. [9] Kilikuwa mraba kilipokunjwa. Walikifanya kile kifuko cha kifuani,
kinapokunjwa, shubiri moja urefu wake na shubiri moja upana wake. [10] Kisha

wakakijaza kwa mistari minne ya mawe. Mstari wa zabarijadi, topazi na zumaridi
ulikuwa mstari wa kwanza. 11 Nao mstari wa pili ulikuwa feruzi, yakuti na yaspi.
12 Nao mstari wa tatu ulikuwa jiwe la leshemi, akiki na amethisti. 13 Nao mstari
wa nne ulikuwa krisolito na shohamu na yashefi. Yaliwekwa katika mapambo ya
dhahabu katika mahali pake. 14 Na mawe hayo yalikuwa kulingana na majina ya
wana wa Israeli. Yalikuwa kumi na mawili kulingana na majina yao, kwa michongo
ya muhuri, kila moja kulingana na jina lake kwa ajili ya yale makabila kumi na
mawili. 15 Nao wakafanya juu ya kile kifuko cha kifuani minyororo yenye mashada,
msokoto wa kamba, wa dhahabu safi. 16 Kisha wakafanya mapambo mawili ya
dhahabu na pete mbili za dhahabu na kuziweka hizo pete mbili kwenye ile miisho
miwili ya kile kifuko cha kifuani. 17 Baada ya hilo wakapitisha zile kamba mbili
za dhahabu kwenye zile pete mbili zilizo kwenye miisho ya kile kifuko cha kifuani.
18 Nao wakapitisha ile miisho miwili ya zile kamba mbili kwenye yale mapambo
mawili. Halafu wakaiweka juu ya vile vipande vya begani vya naivera, mbele yake.
19 Kisha wakafanya pete mbili za dhahabu na kuziweka kwenye ile miisho miwili
ya kile kifuko cha kifuani kwenye upindo wake ulio upande unaoelekea ile efodi
upande wa ndani. 20 Halafu wakafanya pete mbili za dhahabu na kuziweka juu
ya vile vipande viwili vya begani vya efodi upande wake wa chini, sehemu yake
ya mbele, karibu na mahali pake pa kuungania, juu ya ule mshipi wa naivera.
21 Mwishowe wakakifunga kile kifuko cha kifuani kwa pete zake kwenye zile pete
za efodi kwa uzi wa bluu, ili kipate kuwa juu ya mshipi wa efodi na kile kifuko
cha kifuani kisiondoke juu ya efodi, kama vile Yahweh alivyokuwa amemwamuru
Musa. 22 Bezaleli akafanya lile koti la naivera, lote la uzi wa zambarau, kazi ya
mshonaji. 23 Na sehemu wazi ya hilo koti ilikuwa katikati yake, kama sehemu wazi
ya vazi la chuma. Sehemu hiyo iliyo wazi ilikuwa na ukingo kuizunguka pande zote
ili isiraruke. 24 Halafu wakafanya kwenye upindo wa hilo koti makomamanga ya uzi
wa bluu na sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya
kochinili, vilivyosokotwa pamoja. 25 Wakafanya kengele za dhahabu safi na kuziweka
kengele hizo katikati ya makomamanga kwenye upindo wa lile koti kuzunguka pande
zote, katikati ya makomamanga; 26 kengele na komamanga, kengele na komamanga
kwenye upindo wa hilo koti kuzunguka pande zote, kwa ajili ya kuhudumu, kama
vile Yahweh alivyokuwa amemwamuru Musa. 27 Kisha wakafanya zile kamba za
kitani bora, kwa ajili ya Haruni na wanawe. 28 Na kile kilemba cha kitani bora na
yale mavalio ya kichwani ya mapambo ya kitani bora na zile suruali za kitani bora
kilichosokotwa, 29 na ule ukumbuu wa kitani bora kilichosokotwa na uzi wa bluu na
sufu iliyotiwa rangi ya zambarau na kitambaa chenye rangi nyekundu ya kochinili,
kazi ya mfumaji, kama vile Yahweh alivyokuwa amemwamuru Musa. 30 Mwishowe
wakafanya lile bamba linalong'aa, ishara takatifu ya wakfu, kutokana na dhahabu
safi na kuandika juu yake maandishi kwa mchongo wa muhuri: "Utakatifu kwa
Yahweh. " 31 Kisha wakalitia uzi wa bluu ili waliweke juu ya kile kilemba upande wa
juu. Kama vile Yahweh alivyokuwa amemwamuru Musa. 32 Basi kazi ya ile maskani
ya hema la mkutano ikafikia mwisho wake. Kwa maana wana wa Israeli waliendelea
kufanya kulingana na yote ambayo Yahweh alikuwa amemwamuru Musa. 33 Nao
wakaileta maskani kwa Musa, lile hema pamoja na vyombo vyake vyote, kulabu
zake, viunzi vyake vya mbao, miti yake na nguzo zake na vikalio vyake, 34 na kifuniko
chake cha ngozi za kondoo-dume zilizotiwa rangi nyekundu na kifuniko chake cha
ngozi za sili na pazia la kisitiri, 35 na sanduku la ushuhuda na miti yake na kifuniko.
36 Wakaleta meza, vyombo vyake vyote, na ule mkate wa wonyesho, 37 kile kinara
cha taa cha dhahabu safi, taa zake, ule mstari wa taa, na vyombo vyake vyote
na yale mafuta ya kuangazia taa, 38 na madhabahu ya dhahabu na yale mafuta

yanayotumiwa kutia mafuta na ule uvumba uliotiwa manukato na kile kisitiri kwa
ajili ya mwingilio wa hema, 39 ile madhabahu ya shaba na kile kiunzi chake cha shaba,
miti yake na vyombo vyake vyote, ile beseni na kinara chake, 40 Wakaleta mapazia ya
ua, nguzo zake na vikalio vyake na kile kisitiri+ kwa ajili ya lango la ua, kamba zake za
hema na misumari yake ya hema na vyombo vyote kwa ajili ya utumishi wa maskani,
kwa ajili ya hema ya kukutania. 41 Wakaleta yale mavazi yaliyofumwa kwa ajili ya
kuhudumu katika patakatifu, yale mavazi matakatifu kwa ajili ya Aruni kuhani na
mavazi ya wanawe ya kutumikia wakiwa makuhani. 42 Kulingana na yote ambayo
Yahweh alikuwa amemwamuru Musa, hivyo ndivyo wana wa Israeli walivyoufanya
utumishi wote. 43 Naye Musa akaiona ile kazi yote, na, tazama, walikuwa wameifanya
kama vile Yahweh alivyokuwa ameamuru. Hivyo ndivyo walivyokuwa wamefanya.
Basi Musa akawabariki.

# 40

1 Kisha Yahweh akasema na Musa na kumwambia, 2 "Siku ya kwanza ya mwezi wa
kwanza ya mwaka lazima wewe uandae hema la kukutania. 3 Utaweka sanduku
la ushuhuda ndani yake, na utaziba sanduku kwa pazia. 4 Utaleta ndani meza
na kuandaa kwa mpangilio vitu vyake. Kisha utaleta kinara cha taa na kuandaa
taa. 5 Nawe utaweka madhabahu ya dhahabu ya uvumba mbele ya sanduku la
ushuhuda, na utaweka pazia katika mwingilio wa hema la kukutania. 6 Utaweka
madhabahu kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa mbele ya mwingilio wa hema ya
kukutania. 7 Utaweka ile saani kubwa katikati ya hema la kukutania na madhabahu
na utaweka maji ndani yake. 8 Uandae nyuani inayoizunguka, na utundike pazia
katika mwingilio wa nyuani. 9 Lazima uchukuwe mafuta ya upako na upake hema
la kukutania na kila kitu kilichopo ndani yake. Lazima uitenge na samani zake
kwangu; kisha itakuwa takatifu. 10 Lazima upake mafuta madhabahu ya sadaka
ya kuteketezwa na vyombo vyake. Lazima utenge madhabhu kwa ajili yangu na
itakuwa takatifu kwangu. 11 Upake mafuta beseni la shaba na sakafu yake na uitenge
kwa ajili yangu. 12 Umlete Aruni na wanae kwa mwingilio wa hema la kukutania na
uwaoshe wote kwa maji. 13 Utamfunika Aruni kwa mavazi yaliyo tengwa kwa ajili
yangu, mpake mafuta na umtenge ili anitumikie kama kuhani. 14 Utawaleta wana
wake na kuwafunika kwa nguo nzito. 15 Utawapaka mafuta kama ulivyo mpaka baba
yao ili wanitumikie kama makuhani. Upako wao utawafanya makuhani wa kudumu
vizazi vyote vya watu wao." 16 Hivi ndivyo Musa alivyo sema; alifuata yote Yahweh
aliyo muamuru. Alifanya vitu vyote hivi. 17 Hivyo hema la kukutania liliandaliwa
siku ya kwanza ya mwezi wa mwaka wa pili. 18 Musa aliandа hema la kukutania,
akaeka sakafu zake sehemu yake, akaanda fremu zake, akashikisha chuma zake, na
akaanda minara na nguzo zake. 19 Alitandaza mfuniko juu ya hema la kukutania
na kuweka hema juu yake, kama Yahweh alivyo muamuru. 20 Alichukuwa amri za
agano na kuweka kwenye sanduku. Pia aliweka nguzo kwenye sanduku na kuweka
mfuniko wa kiti cha rehema. 21 Aliichukuwa sanduku na kuweka ndani ya hema
la kukutania. Aliandaa pazia ili lizibe sanduku la ushuhuda, kama Yahweh alivyo
muamuru. 22 Alieka meza kwenye hema la kukutania, kwa upande wa kaskazini
mwa hema la kukutania, nje ya pazia. 23 Alieka mkate kwa mpangilio katika meza
ya Yahweh, kama Yahweh alivyo amuru. 24 Alieka kinara cha taa kwenye hema la
kukutania, upande wa pili wa meza, kusini mwa hema la kukutani. 25 Aliwasha
taa mbele za Yahweh, kama Yahweh alivyo muamuru. 26 Aliweka madhabahu ya
dhahabu ya uvumba ndani ya hema la kukutania mbele ya pazia. 27 Alichoma
uvumba wa manukato hapo, kama Yahweh alivyo muamuru. 28 Alitundika pazia
katika hema ya kukutania. 29 Aliweka madhabahu ya sadaka ya kuteketeza katika

hema ya kukutania. Aliitolea sadaka ya kuteketeza na sadaka ya unga, kama Yahweh
alivyo muamuru. 30 Aliweka beseni katikati ya hema ya kukutunia na madhabahu, na
maji ya kuoshea. 31 Musa, Aruni, na wanae waliosha mikono yao na miguu kwenye
beseni 32 muda wowote walipoenda kwenye hema ya kukutania na muda wowote
walipoenda kwenye madhabahu. Walijisafisha, kama Yahweh alivyo muamuru Musa.
33 Musa alianda nyuani nyuma ya hema ya kukutania na madhabahu. Alianda
pazia katika mwingilio wa nyuani. Katika hili, Musa alimaliza kazi. 34 Kisha wingu
likafunika hema ya kukutania, na utukufu wa Yahweh ukafunika hema ya kukutania.
35 Musa hakuweza kuingia hema ya kukutania kwasababu wingu lilikuwa juu yake,
na kwasababu utukufu wa Yahweh ulijaza hema ya kukutania. 36 Muda wowote
wingu lilipo chukuliwa juu kutoka hema ya kukutania, watu wa Israeli waliendelea
na safari yao. 37 Lakini kama wingu haliku nyanyuka juu kutoka hema ya kukutania,
kisha basi watu hawaku safiri. Walibaki hadi siku lilipo nyanyuliwa juu. 38 Kwa kuwa
wingu la Yahweh lilikuwa juu ya hema ya kukutania mchana, na moto wake ulikuwa
juu yake usiku, wazi kwa watu wote wa Israeli kipindi chote cha safari yao.

# Mambo ya Walawi

1 Mungu alimwita Musa na alisema naye kutoka kweye hema la kukutania,
akasema, 2 “Sema na wana wa Israeli na uwaambie, 'Mwanaume yeyote miongoni
mwenu akileta sadaka kwa Bwana, aleta kama matoleo katika wanyama wako, iwapo
mifugo au katika kundi.” 3 Kama matoleo yake ni ya sadaka ya kutekezwa kutoka
katika kundi, atatoa dume asiyekuwa na kasoro. Atamtoa katika mlango wa kuingilia
katika hema ya kukutania, ili iwe imekubaliwa mbele za Bwana. 4 Ataweka mikono
yake kichwani pa sadaka ya kuteketezwa, na ndipo itakuwa imekubaliwa badala yake
kufanya upatanisho kwa ajili yake mwenyewe. 5 Ndipo atapaswa kuchinja ng'ombe
mbele ya Bwana. Watoto wa Aroni, makuhani wataleta damu na kuinyunyizia katika
madhabahu iliyo katika mlango wa kuingilia katika hema la kukutania. 6 Ndipo
ataichuna sadaka ya kuteketezwa na kuikata vipande. 7 Kisha wana wa Haruni
kuhani wataweka moto katika madhabahu na kuweka kuni ili kuchochea moto.
8 Wana wa Haruni, makuhani wataweka vipande, kichwa na mafuta, watazipanga
juu ya kuni zilizoko juu ya moto ulio madhabahuni. 9 Lakini matumbo yake na
miguu lazima ataiosha kwa maji. Kisha kuhani atateketeza kila kitu kilicho juu
ya madhabahu kama sadaka ya kuteketeza. Italeta harufu nzuri sana kwangu;
itakuwa sadaka iliyotolewa kwa moto kwa ajili yangu. 10 Kama sadaka kwa ajili
ya sadaka ya kuteketeza kutoka kundi, kondoo au mbuzi, lazima atoe dume asiye na
kasoro. 11 Lazima atamchinja juu ya madhabahu iliyo katika upande wa kaskazini
mbele ya Bwana. Wana wa Haruni makuhani, watanyunyiza damu kila upande
wa madhabahu. 12 Kisha ataikata katika vipande, pamoja na kichwa na mafuta
yake, kuhani atavipanga juu ya kuni zilizo katika moto ulio madhabahuni, 13 lakini
matumbo yake na miguu yake lazima ioshwe kwa maji. Kisha kuhani atatoa yote
na kuiteketeza juu ya madhabahu. Ni sadaka ya kuteketezwa, italeta harufu nzuri
kwa ajili ya Bwana; itakuwa sadaka ya Bwana iliyotolewa kwa moto. 14 Kama sadaka
yake kwa Bwana itakuwa ni sadaka ya kuteketezwa ni ndege, ndipo ataleta kama
sadaka yake aidha ni huwa au kinda la njiwa. 15 Kuhani atailеta madhabahuni,
atamnyonga kichwa chake, na kuiteketeza juu ya madhabahu. Kisha damu yake
itachuruzishwa juu ya pande za madhabahu. 16 Kisha atakiondoa kibofu chake
pamoja na uchafu wake, na kukiweka upande wa mashariki mwa madhabahu, katika
sehemu ya majivu. 17 Kisha atapasua mabawa yake, lakini hatagawanya katika
vipande viwili. Kisha Kuhani atamtekeza katika madhabahu, juu ya kuni amabazo
ziko juu ya moto. Itakuwa sadaka ya kuteketezwa, na italeta harufu nzuri sana kwa
Bwana; itakuwa sadaka ya Bwana iliyotolewa kwa moto.

## 2

1 Yeyote akitoa sadaka ya nafaka kwa Bwana, sadaka yake lazima iwe unga safi,
na atamwaga mafuta juu yake na kuweka ubani juu yake. 2 Atachukua sadaka
kwa wana wa Haruni, makuhani na pale kuhani atachukua konzi moja ya unga
safi pamoja na mafuta na ubani. Kisha kuhani atateketeza hiyo sadaka juu ya
madhabahu kuwa shukrani kwa uzuri wa Bwana. Italeta harufu nzuri sana kwa
Bwana, itakuwa sadaka ya Bwana iliyotolewa kwa moto. 3 Unga wowote uliobaki
utakuwa ni wa Haruni na watoto wake. Ni takatifu sana kwa Bwana iliyotolewa
sadaka kwa Bwana kwa moto. 4 Kisha utakapotoa sadaka ya unga bila chachu
iliyookwa kweye kiokeo, itakuwa mkate lainiya unga safi uliochanganywa na mafuta,
au mkate mgumu usiokuwa na chachu, ambao umesambazwa na mafuta. 5 Kama

matoleo yako ya nafaka yameokwa na kikaango cha chuma ni lazima iwe unga safi
bila chachu uliochanganywa na mafuta. 6 Utagawanya katika vipande na kumwaga
mafuta juu yake. Hii ni sadaka ya nafaka. 7 Kama sadaka yako ya nafaka imepikwa
katika kikaango, ni lazima iwe imetengenezwa kwa unga safi na mafuta. 8 Utaleta
matoleo ya nafaka yaliyotengenezwa kwa vitu hivi kwa Bwana, italeta kwa kuhani,
ambaye ataleta mbele ya madhabahu. 9 Ndipo kuhani atachukua baadhi ya sadaka
ya nafaka ya shukrani ya Bwana, ataitekeza katika madhabahu. Itakuwa sadaka
ya kuteketezwa kwa moto, italeta harufu nzuri kwa Bwana. 10 Itakayobaki sadaka
ya nafaka itakuwa ya Haruni na wanawe. Itakuwa takatifu kamili ya Bwana kutoka
matoleo kwa Bwana yatolewayo kwa moto. 11 Sadaka ya nafaka itolewayo kwa Bwana
isiwe na chachu, hautatekeza chachu wala asali kama matoleo yatakayotekezwa kwa
moto kwa ajili ya Bwana. 12 Utayatoa kwa Bwana kama mazao ya kwanza, lakini
hayatatumika kama matoleo ya harufu nzuri ya moto juu ya madhabahu. 13 Utaweka
chumvi katika kila matoleo yako ya nafaka. Usipungukie chumvi ya agano la Bwana
katika matoleo yako ya unga. Matoleo yako yote hayatapungukiwa na chumvi.
14 Kama ukitoa matoleo ya nafaka ya mazao ya kwanza kwa Bwana, utatoa nafaka
mbichi yaliyookwa kwa moto, na yaliyopondwa. 15 Lazima utaweka mafuta na ubani
juu yake. Haya ni matoleo ya nafaka. 16 Kuhani atatoa sehemu ya nafaka iliyopondwa
na mafuta na ubani, kama sadaka ya shukrani itolewayo kwa uzuri wa Bwana. Hii
ni sadaka ya Bwana inayotolewa kwa moto.

# 3

1 Kama mtu atoa dhabihu ambayo ni matoleo ya amani ya mnyama kutoka
katika kundi, dume au jike, lazima atatoa mnyama asiyena kasoro mbele ya Bwana.
2 Ataweka mikono yake juu ya sadaka yake na atamchinja mbele ya mlango wa hema
ya kukutania. Kisha wana wa Haruni makuhani watanyunyizia damu yake katika
pande za madhabahu. 3 Mtu akitoa dhabihu ya amani itolewayo kwa moto kwa
ajili ya Bwana. Mafuta yanayofunika au yanayoungana na hizo sehemu za ndani,
4 figo mbili na mafuta yaliyofunika kiunoni na yanayozunguka ini, pamoja na figo
atayatoa pamoja. 5 Wana wa Haruni watayachoma hayo katika madhabahu pamoja
na sadaka ya kutekezwa, juu ya kuni zilizo kwenye moto. Zitaleta harufu nzuri mbele
ya Bwana; itakuwa sadaka ya itolewayo kwake kwa moto. 6 Kama dhabihu ya amani
ya mtu itolewayo kwa Bwana ni kutoka katika mifugo ni mbuzi au kondoo ni dume
au jike, atatoa dhabihu isiyo na kasoro. 7 Kama atatoa mwanakondoo kwa ajili ya
dhabihu yake, atamtoa mbele za Bwana. 8 Ataweka mkono wake juu ya ya kichwa
cha dhabihu yake na atamchinja mbele ya hema ya kukutania. Ndipo wana wa
Haruni watanyunyizia damu pande za madhabahu. 9 Mtu akitoa sadaka ya dhabihu
ya amani kama sadaka ya kusogezwa kwa moto kwa Bwana. Mafuta, mafuta ya mkia
yatakatwa hapo karibu na mfupa wa kiuno, na mafuta yanayofunika matumbo na
mafuta yaliyo katika matumbo, 10 na figo zote mbili na mafuta yanayofunika yaliyo
karibu na kiuno kitambi kilicho karibu na ini na figo ataziondoa zote. 11 Na kuhani
atayatekeza yote kwa moto katika madhabahu kama sadaka ya chakula isogezwayo
kwa moto kwa Bwana. 12 Kama matoleo ya mtu ni mbuzi, ndipo ataitoa mbele ya
Bwana. 13 Ataweka mikono yake juu ya kichwa cha mbuzi na atamchinja mbele ya
hema ya kukutania. Ndipo wana wa Haruni watanyunyizia damu pande zote za
madhabahu. 14 Mtu akitoa dhabihu kwa Bwana kwa njia ya moto. Ataondoa mafuta
yanayozunguka matumbo, na mafuta yote yanayozunguka matumbo. 15 Ataondoa
pia figo mbili na mafuta yanayozunguka, ambayo yanazunguka kiuno na kitambi cha
maini pamoja na figo. 16 Kuhani atateketeza yote juu ya madhabahu kama matoleo
ya chakula yatolewayo kwa moto, ni sadaka ya kuleta harufu nzuri sana. Mafuta

yote ni ya Bwana. 17 Itakuwa ni amri ya kudumu kwa kizazi cha watu katika maeneo
yote mtakapotengeneza makazi, kwamba hamtakula mafuta au damu.”'

# 4

1 Bwana alisema na Musa na kumwambi, 2 “Waambie wana wa Israeli 'mtu
yeyote akifanya dhambi bila kukusudia, kufanya chochote ambacho Bwana ameagiza
kutofanya, na kama akifanya chochote kilichozuiliwa, yafuatayo lazima yatatendeka.
3 Kama ni kuhani mkuu aliyetenda dhambi na kuleta hatia kwa watu, atatoa dume
asiyekuwa na kasoro kwa Bwana kwa ajili ya dhambi aliyotenda kama sadaka
ya dhambi. 4 Ataleta dume mbele ya mlango wa hema ya kukutania mbele ya
Bwana, ataweka mikono juu ya dume, na atamchinja huyo dume mbele za Bwana.
5 Kuhani aliyewekewa mafuta atachukua damu ya dume na kuileta mbele ya hema
ya kukutania. 6 Kuhani atazamisha kidole chake katika damu na kuinyunyiza
mara saba mbele za Bwana, mbele ya pazia la mahali pa takatifu. 7 Na kuhani
ataweka kiasi cha damu ya huyo dume juu ya pembe za madhabahu ya kuvukizia
uvumba mbele za Bwana, katika hema ya kukutania na ataimwaga yote iliyobaki
chini ya madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa, iliyo mahali pa kuinglia katika
hema ya kukutania. 8 Atakata mafuta yote ya dume wa sadaka ya dhambi, mafuta
yanayofunika matumbo na mafuta yote yaliyo katika matumbo, 9 figo mbili na mafuta
yaliyopo pamoja nazo, yaliyo karibu na kiuno na kitambi cha maini pamoja na hizo
figo. 10 Ataondoa zote vile vile kama yanavyoondolewa katika dume wa sadaka ya
dhabihu ya amani. Kuhani atatekeza sehemu hizo katika madhabahu ya sadaka za
kuteketezwa. 11 Ngozi ya dume na mabaki yoyote ya nyama, pamoja na kichwa chake,
miguu yake, matumbo yake na mavi yake, 12 mabaki yote ya dume atayachukua
nje ya mji mahali palipo safi, mahali wanapomwaga majivu; watateketeza sehemu
zote juu ya kuni. Watateketeza sehemu zote mahali wanapomwaga majivu. 13 Kama
mkutano wote wa wana wa Israeli wakitenda dhambi bila kukusudia, na mkutano
hawatakumbuka kwamba wametenda dhambi, na kufanya vile Bwana aliagiza
wasifanye na wakajisikia hatia. 14 Na dhambi waliyofanya ikajulikana, mkutano
watatoa ng'ombe dume mchanga kuwa sadaka ya dhambi watamleta mbele ya hema
ya kukutania. 15 Wazee wa mkutano wataweka mikono yao juu ya kichwa cha
ng'ombe mbele za Bwana, na ng'ombe atachinjwa mbele za Bwana. 16 Kuhani
aliyetiwa mafuta ataleta damu ya ng'ombe katika hema ya kukutania, 17 kuhani
atachovya kidole chake katika damu na kuinyunyizia mara saba mbele za Bwana
mbele ya pazia. 18 Ataweka kiasi cha damu katika pembe za madhabahu mbele
za Bwana iliyo katika hema ya kukutania na ataimwaga damu yote chini ya
madhabahu ya sadaka ya kuteketezwa, iliyo katika mlango wa kuingilia katika hema
ya kukutania. 19 Atakata mafuta yote na kuyatekeza katika madhabahu. 20 Hivyo
ndivyo atakavyomfanya huyo ng'ombe, kama alivyomfanya ng'ombe wa sadaka ya
dhambi, atamfanyia vivyo hivyo huyu ng'ombe, kuhani atawafanyia upatanisho
watu nao watasamehewa. 21 Atamchukua huyo ng'ombe nje ya mji na kumteketeza
kama alivyomteketeza ng, ombe wa kwanza. Hii ni sadaka ya dhambi kwa ajili
ya mkutano. 22 Mtawala akitenda dhambi bila kukusudia kufanya moja ya yale
Bwana Mungu wake ameagiza kutotenda, na anajisikia hatia 23 na kama dhambi
yake aliyotenda anaifahamu, ataleta dhabihu yake mbuzi mme asiye na kasoro.
24 Ataweka mkono wake juu ya kichwa cha mbuzi na kumchinja mahali ambapo
huchinja sadaka ya kuteketezwa mbele za Bwana. Hii ni sadaka ya dhambi. 25 Kuhani
atachukua damu ya sadaka ya dhambi kwa kidole chake na kuiweka juu ya pembe za
madhabahu kwa dhabihu ya kuteketezwa, na atamwaga damu chini ya madhabahu
ya dhabihu ya kuteketezwa. 26 Atateketeza mafuta yote katika madhabahu, kama

vile mafuta ya dhabihu ya sadaka ya amani, Kuhani atafanya upatanisho kwa ajili ya
mtawala kulingana na dhambi yake, na mtawala atakuwa amesamehewa. 27 Kama
yeyote wa watu wa kawaida akitenda dhambi bila kukusudia, kufanya vitu ambavyo
Bwana ameagiza kutokufanywa na kama ana hatia, 28 ndipo dhambi yake aliyoitenda
ikajulikana kwake, ndipo ataleta mbuzi mke asiyekuwa na kasoro awe dhabihu
kwa ajili ya dhambi zake alizotenda. 29 Ataweka mikono yake juu ya sadaka ya
dhambi na kuchinja sadaka ya dhambi mahali pa sadaka ya kuteketezwa. 30 Kuhani
atachukua kiasi cha damu kwa kidole chake na kuweka katika pembe za madhabahu
ya dhabihu ya kuteketezwa. Damu yote iliyobaki ataimwaga chini ya madhabahu.
31 Atayaondoa mafuta yote, kama alivyoondoa mafuta katika dhabihu ya amani.
Kuhani ataiteketeza katika madhabahu ili kuwa harufu nzuri kwa Bwana. Kuhani
atafanya upatanisho kwa mtu, na atasamehewa. 32 Kama mtu ataleta mwanakondoo
kama dhabihu yake kwa sadaka ya dhambi, ataleta jike asiye na kasoro. 33 Ataweka
mikono kichwani mwa sadaka ya dhambi na atamchinja kuwa sadaka ya dhambi
mahali wanapochinjwa sadaka ya kuteketezwa. 34 Kuhani atachukua baadhi ya damu
ya sadaka ya dhambi kwa kidole chake na kuweka katika pembe za madhabahu
kwa ajili ya sadaka za kuteketezwa, na ataimwaga damu yote chini ya madhabahu.
35 Ataondoa mafuta yote, kama akatavyo mafuta ya mwanakondoo dhabihu ya
sadaka ya amani na kuhani ataiteketeza juu ya madhabahu juu ya sadaka ya Bwana
itolewayo kwa moto. Kuhani ataleta upatanisho kwa dhambi aliyoifanya, naye
atasamehewa.

# 5

1 Kama mtu atatenda dhambi kwa sababu hakusema ukweli wakati alipotakiwa
kutoa ushahidi fulani kuhusu kile alichotakiwa, ameona au kufahamu habari zake,
yeye anastahili adhabu. 2 Au mtu akigusa kitu chochote ambacho Mungu amekitaja
kuwa ni najisi hata kama ni mzoga wa wanyama wa porini au ni mzoga wa wanyama
wa kufugwa au wataambaao hata kama mtu huyo hakukusudia kumgusa, yeye ni
najisi na mwenye hatia. 3 Au amegusa kitu chochote kilicho kichafu, kwa vyovyote
kama hakujua, ndipo atakuwa na hatia akijua vile. 4 Au kama yeyote akiapa bila
kufikiri kwa midomo yake kufanya ubaya, au kufanya vyema kwa vyovyote vile mtu
ameapa kwa haraka atakapotambua atakuwa na hatia kwa vitu hivyo. 5 Mtu yeyote
akiwa na hatia kwa vitu hivi, lazima akiri kwa yoyote dhambi aliyotenda. 6 Ndipo
atakapoleta sadaka yake ya hatia mbele za Bwana kwa dhambi aliyokwisha tenda.
Ataleta kondoo jike au mbuzi kutoka katika kundi lake kuwa matoleo ya dhambi,
kuhani atafanya upatanisho kuhusu dhambi yake. 7 Kama hataweza kununua mwana
kondoo ataleta kama sadaka ya hatia, hua wawili au makinda mawili ya njiwa kwa
Bwana, mmoja kwa sadaka ya dhambi na mwingine ni sadaka ya kutekeketezwa.
8 Atawaleta kwa kuhani, wa kwanza atatoa kwa ajili ya sadaka ya dhambi. Atamvunja
shingo yake lakini ataacha kichwa chake kinaning'inia wala hataiondoa kabisa shingo
yake katika mwili. 9 Ndipo atanyunyizia damu yake katika sehemu za madhabahu,
na damu inayobaki ataimwaga chini ya madhabahu. Hii ni dhabihu ya dhambi.
10 Ndipo ataoa ndege wa pili kama sadaka ya kuteketezwa kama ilivyoelekezwa, na
kuhani atafanya upatanisho kwa ajili ya dhambi alizokwisha kufanya, na huyo mtu
atakuwa amesamehewa. 11 Lakini kama hataweza kununua hua wawili au makinda
ya njiwa mawili, ndipo ataleta kama dhabihu ya dhambi zake sehemu ya kumi ya
unga laini kama sadaka ya dhambi. Asiweke mafuta wala ubani juu yake, kwa kuwa
ni sadaka ya dhambi. 12 Atauleta kwa kuhani, na kuhani atachukua konzi moja
ya unga kama ukumbusho wa wema wa Bwana na atauweka juu ya madhabahu
na kuteketeza juu ya sadaka za kuteketezwa kwa moto kwa ajili ya Bwana. Hii ni
sadaka ya dhambi. 13 Kuhani atafanya upatanisho kwa dhambi yoyote aliyofanya

mtu yeyote, mtu huyo atasamehewa. Na sadaka inayobaki itakuwa ya kuhani, kama
ilivyo sadaka ya nafaka.'" 14 Bwana akamwambia Musa, akasema, 15 "Kama mtu
akikiuka amri na kufanya dhambi kinyume na mambo matakatifu ya Bwana, lakini
akifanya bila kukusudia ataleta sadaka ya hatia kwa Bwana. Sadaka hii itakuwa
ni kondoo dume asiye na kasoro kutoka katika kundi; thamani yake halisi kifedha
kulingana na shekeli ya mahali patakatifu, kama sadaka ya hatia. 16 Lazima atalipa
kwa Bwana kwa kile alichokosa kulingana na kitakatifu, na ataongezea moja ya
tano na kumpa kuhani. Ndipo kuhani ataweka upatanisho kwa ajili yake pamoja na
kondoo wa sadaka ya hatia, na mtu atakuwa amesamehewa. 17 Kama mtu akitenda
dhambi kwa kufanya kile ambacho Bwana aliagiza kisifanyike, hata kama hakujuwa,
atakuwa na hatia na ataibeba hatia yake. 18 Lazima ataleta kondoo dume asiye na
kasoro kutoka katika kundi, anayestahili thamani ya fedha, kama sadaka ya hatia
kwa kuhani. Ndipo kuhani atafanya upatanisho kulingana na dhambi aliyotenda,
ambayo hakujua atakuwa amesamehewa. 19 Ni sadaka ya hatia, na amekuwa na
hatia mbele za Bwana."

# 6

1 Bwana alisema na Musa kumwabia, 2 "Kama mtu akifanya dhambi na kuvunja
amri kinyume na Bwana, kama kujihusisha na uongo dhidi ya jirani yake kuhusu kitu
fulani cha kutokuwa mwaminifu, au kama akidanganya au kuiba au amemdhurumu
jirani. 3 Au akiokota kitu fulani ambacho jirani yake amepoteza na kusema uongo
kuhusu hicho, na kuapa kwa uongo au kwa mambo kama haya ambayo watu
wanaweza kutenda dhambi. 4 Ndipo itakuwa hivi, kama ametenda dhambi na hatia,
kwamba lazima akirudishe kwa vyovyote alichoiba au kudanganya au amedhurumu
au kitu kilichopotea naye kukiokota. 5 Au kama amedanganya kwa jambo lolote,
lazima atakirudisha kamilina kuongezea sehemu ya tano kwa kumlipa anayedai,
kwa siku ile anayopatikana na hatia. 6 Ataleta sadka ya hatia kwa Bwana: kondoo
dume asiye na kasoro kutoka katika kundi lake kulingana na thamani yake, kama
sadaka ya hatia kwa kuhani. 7 Kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake mbele
ya Bwana, atakuwa amesamehewa kulingana na chochote kilicho mfanya kuwa na
hatia." 8 Ndipo Bwana alisema na Musa kumwambia, 9 "Mwagize Haruni na wanawe,
kusema, 'hii ni sheria ya sadaka ya kuteketezwa: Sadaka ya kuteketezwa lazima
iwe juu ya makaa ya madhabahu usiku wote hata asubuhi, na moto wa madhabahu
utaendelea kuwaka. 10 Kuhani atavaa nguo zake za kitani na atavaa nguo za kitani
ndani yake. Atatoa majivu yaliyobaki baada ya moto kutekeza sadaka ya kuteketezwa
juu ya madhabahu, na ataweka majivu pembeni mwa madhabahu. 11 Atavua mavazi
haya na kuvaa mavazi mengine ili kuchukua majivu nje ya kambi na kupeleka
mahali palipo safi. 12 Moto katika madhabahu utaendelea kuwaka. Usizimike, na
kuhani ataongeza kuni kila asubuhi. Atapanga juu yake sadaka ya kuteketezwa
kama inavyotakiwa, na atateketeza juu yake mafuta ya sadaka ya amani. 13 Moto
lazima utaendelea kuwaka katika madhabahu, kamwe usizimike. 14 Hii ni sheria ya
sadaka ya nafaka. Wana wa Haruni watatoa mbele ya Bwana katika madhabahu.
15 Kuhani atachukua konzi ya unga laini wa sadaka ya nafaka na mafuta na ubani
ambao uko juu ya sadaka ya nafaka, atateketeza juu ya madhabahu kuleta harufu
nzuri ya shukrani ya kumpendeza Bwana. 16 Haruni na wanae watakula sadaka
inayobaki, italiwa bila kutiwa chachu mahali patakatifu. Watakula katika ua ya hema
ya kukutania. 17 Haitaokwa pamoja na chachu. Nimewapa kama sehemu ya sadaka
yangu itolewayo kwa moto, ni takatifu sana, kama sadaka ya dhambi na sadaka ya
hatia. 18 Kwa nyakati zote zijazo kupitia watu wa kizazi chako, mwanaume yeyote
mzaliwa kutoka kwa Haruni aweza kula ni sehemu yake, ichukuliwayo katika sadaka

ya Bwana kwa moto. Yeyote anayeigusa atakuwa mtakatifu." 19 Bwana aliongea
tena na Musa kumwambia, 20 "Hii ni sadaka ya Haruni na wanawe ambayo watatoa
kwa Bwana katika siku ambayo kila mwana atawekwa wakfu: sehemu ya kumi
ya efa ya unga laini kama kawaida sadaka ya nafaka nusu yake asubuhi na nusu
yake jioni. 21 Itatengenezwa na mafuta katika kikaango, utaileta ikiwa imeandaliwa
imeokwa katika vipande utatoa sadaka ya nafaka ili kuleta harufu nzuri kwa Bwana.
22 Mwana wa Kuhani Mkuu atakayekuwa Kuhani Mkuu mpya kutoka miongoni mwa
wanawe ataitoa. Kama amri ya milele, yote itateketezwa kwa Bwana. 23 Kila sadaka
ya nafaka ya kuhani itatekezwa yote. Haitaliwa kamwe." 24 Bwana alisema tena
Musa, kumwambia, 25 "Sema na Haruni na watoto wake kwamba, 'Hii ni sheria
ya sadaka ya dhambi: Sadaka ya dhambi lazima kuchinjwa mahali pa sadaka ya
kuteketezwa itachinjwa mbeleya Bwana. Ni takatifu sana. 26 Kuhani atakayeitoa
kwa ajili ya dhambi ndiye atakayeila. Italiwa mahali patakatifu katika ua wa hema
ya kukutania. 27 Yeyote atakayeigusa nyama yake atakuwa ni mtakatifu na kama
damu itadondokea mavazi yatafuliwa mahali palipodondokewa, mahali patakatifu.
28 Lakini chungu kikipikiwa kitavunjwa, kama imepikiwa katika chombo cha shaba,
lazima kitasuguliwa na kusafishwa kwa maji. 29 Mwanaume yeyote miongoni mwa
makuhani anaweza kula nyama hiyo kwa sababu ni takatifu sana. 30 Na hakuna
sadaka ya dhambi italiwa ambayo damu yake imeletwa katika hema ya kukutania
kufanya upatanisho katika mahali patakatifu. Ni lazima iteketezwe.

# 7

1 Hii ndiyo sheria ya sadaka ya hatia. Kwa sababu hiyo ni sadaka takatifu sana.
2 Ni lazima waichinje sadaka ya hatia mahali panapostali kuchinjwa, na ni lazima
watainyunyiza damu yake pande zote za madhabahu. 3 Mafuta yote yaliyomo ndani
yake yataondolewa: mafuta ya mkiani, mafuta yaliyo sehamu za ndani, 4 zile figo
mbili pamoja na mafuta yaliyo juu yake, yaliyo karibu na kiuno, na yanayofunika
ini—nyama hii yote lazima iondolewe pamoja na hizo figo. 5 Kuhani ataviteketeza
vipande hivi juu ya madhabahu viwe dhabihu iliyofanywa kwa Yahweh kwa moto.
Hii ni sadaka ya hatia 6 Kila mwanaume miongoni mwa familia ya kuhani anaweza
kula sehemu ya sadaka hii. Lakini ni lazima iliwe ndani ya mahali patakatifu kwa
sababu ni takatifu sana. 7 Nayo sadaka ya dhambi ni kama ilivyo sadaka ya hatia.
Ni sheria ileile hutumika kwa zote mbili. Zote ni mali ya kuhani azitumiaye kufanya
upatanisho. 8 Kuhani atoaye sadaka ya kuteketezwa kwa ajili ya mtu yeyote anaweza
kuchuku ngozi ya sadaka hiyo kwa ajili yake mwenyewe. 9 Kila sadaka ya nafaka
inayookwa mekoni, na kila sadaka kama hiyo ipikwayo kaangoni au kwenye sufuria
itakuwa ya kuhani aitoaye. 10 Kila sadaka ya nafaka, ama iwe unga mkavu au
uliochanganywa na mafuta ya zeitu itakuwa ya ukoo wa Aroni kwa usawa. 11 Hii
ndiyo sheria ya dhabihu ya sadaka za amani, ambazo watu watazitoa kwa Yahweh.
12 Iwapo mtu yeyote anaitoa ili kuonyesha shukrani kwa Yahweh, basi ataitoa pamoja
na dhabih uya mikate iliyotengenezwa bila hamira, bali kwa mafuta ya zeituni
yaliyochanganywa na unga lakini bila hamira, na maandazi yaliyotengenezwa bila
hamira, bali yaliyopakwa mafuta juu yake, na mikate miembamba iliyofanywa kwa
unga laini uliochanganywa na mafuta. 13 Kwa kusudi la kutoa shukrani, pia anapaswa
kutoa pamoja na sadaka yake ya amani, vipande vya mikate iliyotiwa hamira. 14 Ni
lazima atatoa moja kila aina ya sadaka hizi kama sadaka iliyoletwa kwa Yahweh.
Nayo itakuwa ya makuhani wanaonyunyizia damu ya sadaka ya amani kwenye
madhabahu. 15 Mtu anayeleta sadaka ya amani kwa kusudi la kutoa shukrani
ni lazima ataila nyama ya sadaka yake siku ya kutoa dhabihu. Hatakiwi kusaza
chochote kilicho cha sadaka hiyo hata asubuhi ya pili. 16 Lakini iwapo dhabihu ya

matoleo yake kusudi lake ni nadhiri, au kwa kusudi la sadaka ya hiari, nyama yake
italiwa siku iyo hiyo aitoapo dhabihu yake, lakini chochote kinachosalia cha sadaka
hiyo kinaweza kuliwa siku inayofuata. 17 Hata hivyo, nyama yoyote ya dhabihu
inayobaki siku ya tatu ni lazima ichomwe moto. 18 Iwapo kipande chochote cha
nyama hiyo ya dhabihu kinachobaki kinaliwa katika siku ya tatu, hakitakubalika,
wala hakitatolewa kwa aliyeitoa. Kitakuwa ni kitu cha kuchukiza, na mtu akilaye
atabeba hatia ya dhambi mwenyewe yake. 19 Nyama yoyote inayogusa kitu kilicho
najisi haitaliwa. Ni lazima ichomwe moto. Na kwa ajili ya nyama inayobaki, yeyote
aliye safi anaweza kuila. 20 Hata hivyo, mtu najisi anayekula nyama kutoka kwenye
dhabihu ya matoleo ya amani ambayo ni ya Yahweh yapasa mtu huyu akatiliwe mbali
kutoka kwa watu wake. 21 Iwapo mtu yeyote anagusa kitu chochote kilichonajisi—iwe
ni unajisi wa binadamu, au wa mnyama aliyenajisi, au wa kitu fulani kilichonajisi na
chenye kuchukiza, na kisha akala baadhi ya nyama ya dhabihu ya sadaka ya amani
iliyotolewa kwa Yahweh, lazima mtu huyo akatiliwe mbali kutoka kwa watu wake.
22 Kisha Yahweh akazungumza na Musa, akisema, 23 "Zungumza na watu wa Israeli
na uwaambie, 'hamruhusiwi kula mafuta ya fahali au kondoo au mbuzi. 24 Mafuta
ya mnyama yoyote afaye peke yake bila ya kuwa dhabihu, au mafuta ya mnyama
yeyote aliyeraruliwa na wanyama pori, yanaweza kutumika kwa makusudi mengine,
lakini hakika hamtayala. 25 Yeyote atakayekula mafuta ya mnyama ambayo watu
wanaweza kuyatoa kuwa dhabihu ya iliyofanywa kwa Yahweh kwa moto, mtu huyo
lazima atakatiliwa mbali kutoka kwa watu wake. 26 Hamtakula damu yoyote katika
mojawapo ya nyumba zenu, ama iwe kutoka kwa ndege au mnyama. 27 Yeyote alaye
damu yoyote, mtu huyo lazima akatiliwe mbali kutoka kwa watu wake.'" 28 Kwa
hiyo Yahweh akazungumza na Musa na akasema, 29 "Zungumza na watu wa Israeli
na uwaambie, 'Yeye atoaye dhabidhu ya sadaka ya amani kwa Yahweh lazima alete
sehemu ya dhabihu yake kwa Yahweh. 30 Mikono yake mwenyewe lazima iilete
hiyo sadaka ifanywayo kwa Yahweh kwa moto. Naye atayaleta hayo mafuta pamoja
na kidari, ili kwamba kidari kiweze kutikiswa kuwa sadaka ya kutikiswa mbele za
Yahweh. 31 Kuhani atayachoma mafuta hayo juu ya madhabahu, lakini kile kidari
kitakuwa mali ya Aroni na uzao wake. 32 Ni lazima utatoa paja la kulia kwa kuhani
kama sadaka iliyotokana na dhabihu ya sadaka yako ya amani. 33 Yule kuhani, mmoja
wa wazao wa Aroni, atoaye damu na mafuta ya sadaka ya amani—ni lazima atapata
paja la kulia kama mgao wake wa sadaka. 34 Kwa kuwa nimetwaa kidari, na paja
la sadaka ya kutikiswa kutoka kwa watu wa Israeli uwe mchango wao, na amepewa
Aroni kuhani na wanawe kuwa mgao wao wa kawaida. 35 Huu ndiyo mgao wa Aroni
na uzao wake utokanao na matoleo yaliyofanywa kwa Yahweh kwa moto, siku ile
Musa alipowaweka wakfu ili kumtumikia Yahweh katika kazi ya kuhani. 36 Huu ndio
mgao ambao Yahweh aliamru waweze kupewa kutoka kwa watu wa Israeli, katika
siku hiyo aliyowatia mafuta ya upako wawe makuhani. Nao utakuwa mgao wao
wa kila siku katika vizazi vyote. 37 Hii ndiyo sheria ya sadaka ya kuteketezwa, ya
sadaka ya nafaka, ya sadaka ya dhambi, ya sadaka ya hatia, ya sadaka ya kuweka
wakfu, na ya dhabihu, ya sadaka za amani, 38 ni sheria ambazo Yahweh alizitoa kwa
Musa kwenye Mlima Sinai siku aliyowaamru watu wa Israeli kutoa dhabihu zao kwa
Yahweh katika jangwa la Sinai.'"

# 8

1 Yahweh akazungumza na Musa, akisema, 2 "Walete Aroni na wanawe pamoja
naye, mavazi na mafuta ya upako, fahali kwa ajili ya sadaka ya dhambi, kondoo dume
wawili, na kikapu cha mkate usio na hamira. 3 Ita kusanyiko lote kwenye ingilio
la hema la kukutania." 4 Kwa hiyo Musa akafanya kama Yahweh alivyomwamru,

nalo kusanyiko lilikuja pamoja mbele ya ingilio la hema la kukutania. Kisha
Musa akaliambia kusanyiko, 5 "Hivi ndivyo alivyotuamru Yahweh tutende." 6 Musa
akamleta Aroni na wanawe na kuwaosha kwa maji. 7 Akamvika Aroni kanzu ya
ndani yenye urefu wa kufika magotini na kumfunga ukumbuu kiunoni mwake,
akamvika joho la nje lenye mikono mirefu na kumvika kile kizibao chenye vipande
viwili tumboni na mgongoni na kukifunga kuzunguka kiunoni mwake kwa mshipi
uliosokotwa kwa ustadi na kukikaza mwilini mwake. 8 Kisha Musa akaweka kifuko
kifuani mwa Aroni, na ndani ya kifuko hicho akaweka Urimu na Thumimu. 9 Na
kisha akamfunga kiremba kichwani, na juu ya kiremba kwa mbele, akaweka bamba
la dhahabu; liwe taji takatifu, kama Yahweh alivyomwamru yeye. 10 Musa akayatwaa
hayo mafuta ya upako, akalipaka lile hema la kukutania na kila kitu kilichokuwamo
ndani yake na kuvitenga kwa ajili ya Yahweh. 11 Akayanyunyiza hayo mafuta juu
ya madhabahu mara saba, na kisha akaipaka mafuta hiyo madhabahu na vyombo
vyake vyote, na sinia la kunawia na kitako chake ili kuvitenga wa ajili ya Yahweh.
12 Akamimina sehemu ya mafuta ya upako juu ya kichwa cha Aroni na kisha
akampaka mafuta ili kumtenga. 13 Musa akawaleta wana wa Aroni na kuwavika kila
mmoja kanzu ya ndani yenye urefu wa kufika magotini. Kila mmoja wao akamfunga
kwa ukumbuu kiunoni mwake na kuwafunga vitambaa vya kitani kichwani pao,
kama vile Yahweh alivyokuwa amemru Musa. 14 Musa akamleta huyo fahali kwa
ajili ya sadaka ya dhambi, naye Aroni na wanawe wakaweka mikono yao juu ya
kichwa cha fahali ambaye wamemelete kwa ajili ya sadaka ya dhambi. 15 Musa
akamchinja, na kisha akachukua sehemu ya damu yake kwa kidole chake na kuiweka
juu ya mpembe za madhabahu, akaitakasa hiyo madhabahu, na kuitenga kwa Mungu,
ambapo kwa kufanya hivyo, aliisababisha madhabahu kuwa sehemu ya kufaa kwa
kufanyia upatanisho. 16 Akachukua mafuta yote yaliyokuwa sehemu za ndani, kile
kiwambo cha ini, zile figo mbili pamoja na mafuta yake, Musa akaichoma hiyo nyama
yote juu ya madhabahu. 17 Lakini yule fahali, ngozi yake, nyama yake na kinyesi
chake, akavichoma nje ya kambi, kama vile Yehweh alivyokuwa amemwamru yeye.
18 Musa akamleta yule konndoo dume kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa, naye
Aroni na wanawe wakaweka mikono yao juu ya kichwa cha huyo kondoo. 19 Musa
akamchinja kondoo na kuinyunyizia damu yake kila upande wa madhabahu. 20 Naye
akamkatakata kondoo vipande vipande na akakiteketeza kichwa chake pamoja na
vile vipande na mafuta. 21 Akaziosha kwa maji zile sehemu za ndani pamoja na
miguu na akamteketeza kandoo mzima juu ya madhabahu. Ilikuwa ni dhabihu ya
kuteketezwa na ilitoa harufu ya kupendeza, sadaka iliyofanywa kwa Yahweh kwa
moto kama vile Yahweh alivyokuwa amemwamru Musa. 22 Kisha Musa akamleta
yule kondoo dume mwingine, kondoo wa kuwekwa wakfu, naye Aroni na wanawe
wakaweka mikono yao juu ya kichwa cha kondoo. 23 Aroni akamchinja, naye Musa
akachukua sehemu ya damu na kuiweka kwenye ncha ya sikio la Aroni la kulia, juu
ya dole gumba la mkono wake wa kulia, na kwenye kidole kikumbwa cha mguu
wake wa kulia. 24 Akawaleta wana wa Aroni, naye akaweka sehemu ya damu
ya kondoo yule kwenye ncha ya sikio lao la kulia, kwenye dole gumba lao cha
mkono wa kulia na kwenye kidole chao kikubwa cha mguu wa kulia. Kisha Musa
akainyunyiza damu ya huyo kila upande wa madhabahu 25 Naye akayatwaa yale
mafuta, mafuta ya mkiani, mafuta liyolikuwa sehemu za ndani, na mafuta yafunikayo
ini, zile figo mbili pamoja na mafuta yake na paja la kulia. 26 Akachukua mkate
mmoja kutoka kwenye kikapu cha mikate isiyo na hamira ambayoo ilikuwa mbele
za Yahweh, akatwaa mkate moja usio na hamira, na mkate mmoja ulioandaliwa
kwa mafuta, na mkate mwemba wa kaki na akaiweka juu ya mafuta na juu ya
paja la kulia la kondoo. 27 Akaiweka yote mikoni mwa Aroni na katika mikono ya

wanawe na kuitikisa mbele za Yahweh kuwa sadaka ya kutikiswa 28 Kisha Musa
akaichukua mikate hiyo kutoka mikononi mwao na kuiteketeza juu ya madhabahu
kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa. Zilikuwa ni sadaka ya kuwekwa wakfu na ilitoa
harufu ya kupendeza. Ilikuwa sadaka iliyofanywa kwa Yahweh kwa moto. 29 Musa
akakichukua kidari na kukitikisa kuwa sadaka ya kutikiswa kwa Yahweh. Ilikuwa ni
mgao wa Musa wa kondoo wa kuwekewa mikono kwa makuhani, Kama vile Yahweh
alivyokuwa amemwamuru yeye. 30 Musa akatwaa sehemu ya mafuta ya upako na
damu iliyokuwa juu ya madhabahu; naye akayanyunyiza haya juu ya nguo za Aroni,
juu ya nguo zake mwenyewe na juu ya nguo za wana wa Aruni waliokua pamoja
naye. Kwa njia hii alimtenga Aroni na nguo zake, na wanawe na nguo zao kwa
ajili ya Yahweh. 31 Kwa hiyo Musa akawambia Aruni na wanawe, “Ipikeni nyama
mbele ya ingilio la hema la kukutania, na hapo mtaila pamoja na mkate ulio kwenye
kikapu cha kuwekwa wakfu, kama ilivyoamriwa, kusema, 'Aroni na wanawe wataila.'
32 Masalio yoyote ya nyama na mikate utayateketeza kwa moto. 33 Na hamtatoka
kwenye ingilio la hema la kukutania kwa muda wa siku saba, hata zitakapotimia siku
za kuwekwa mikono kwenu. Kwa kuwa kwa muda wa siku saba, Yahweh atawaweka
wakfu. 34 Kilichotendeka siku hii— Yahweh ndiye amekiamru kitendekeke ili kufanya
upatanisho kwa ajili yenu. 35 Mtakaa kwenye ingilio la hema la kukutania mchana
na usiku siku saba, nanyi ishikeni amri ya Yahweh ili msije mkafa, kwa sababu hivi
ndivyo ilivyoamriwa. 36 Kwa hiyo Aroni na wanawe wakafanya mambo yote ambayo
Yahweh alikuwa amewaamru kwa kinywa cha Musa.

# 9

1 Katika siku ya nane, Musa akawaita Aroni na wanawe pamoja na wazee wa
Israeli. 2 Akamwambia Aroni, “Twaa ndama dume kutoka kundini kwa ajili ya
sadaka ya dhambi zako, na kondoo dume kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa, wote
wawili wasiwe na dosari, na uwatoe mbele za Yahweh. 3 Zungumza na watu wa
Israeli na uwaambie, 'Twaeni beberu kwa ajili ya sadaka ya dhambi na ndama na
mwana-kondoo, hawa wawili wawe na umri wa mwaka mmoja na bila dosari, ni
kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa; 4 pia twaeni fahali na kondoo dume kwa sadaka
za amani ili kuwatoa mbele za Yahweh, na sadaka za nafaka iliyochanganywa na
mafuta, kwa sababu leo Yahweh atajidhihirisha kwenu. 5 Kwa hiyo wakaleta kwenye
hema la kukutania vyote ambavyo Musa aliagiza, nalo kusanyiko lote la Israeli
likakaribia na kusimama mbele za Yahweh. 6 Kisha Musa akasema, “Hivi ndivyo
Yahweh amewaamru nyinyi mfanye, ili kwamba utukufu wake uweze kuonekana
kwenu. 7 “Musa akamwambia Aroni, “Njoo karibu na Madhabahu na uteo sadaka
yako ya dhambi na sadaka ya kuteketezwa, na kufanya upatanisho kwa ajili ya watu
ili kufanya upatanisho kwa ajili yao kama vile ambavyo Yahweh amekwishaamru.”
8 Kwa hiyo Aroni akaikaribia madhabahu na akamchinja yule ndama kwa ajili ya
sadaka ya dhambi, ambayo ilikuwa kwa ajili yake mwenyewe. 9 Nao wana wa
Aroni wakamletea hiyo damu, naye akakichofya kidole chake kwenye damu na
kuiweka kwenye pembe za madhabahu, kisha akaimwaga damu chini ya kitako cha
madhabahu. 10 Hata hivyo, aliyateketeza hayo mafuta, figo, na mafuta yanafunika
ini juu ya madhabahu kuwa sadaka ya dhambi, kama vile Yahweh alivyokuwa
amemwamru Musa. 11 Na akaiteketeza hiyo nyama pamoja na ngozi nje ya kambi
12 Aroni akaichinja sadaka ya kuteketezwa, nao wanawe wakampa hiyo damu,
ambayo aliinyunza pande zote za madhabahu. 13 Kisha wakampa ile sadaka ya
kuteketezwa, kipande kwa kipande, pamoja na kichwa, naye akaviteketeza juu ya
madhabahu. 14 Akaziosha sehemu za ndani pamoja na miguu na kuziteketeza juu ya
dhabihu ya kuteketezwa juu ya Madhabahu. 15 Aroni akaleta dhabihu ya watu—

mbuzi, kisha akamtoa kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi yao naye akamchinja,
akaitoa dhabihu kwa ajili ya dhambi, kama alivyofanya kwa yule mbuzi wa kwanza.
16 Akaileta sadaka ya kuteketezwa na kuitoa kama Yahweh alivyokuwa ameamru.
17 Akaileta sadaka ya nafaka; akakijaza kiganja chake nafaka na kuiteketeza juu
ya madhabahu, pamoja na sadaka ya asubuhi ya kuteketezwa. 18 Pia akamchinja
fahali na yule kondoo dume, dhabihu kwa ajili ya sadaka ya amani, ambayo ilikuwa
kwa ajili ya watu. Nao wana wa Aronni wakampa damu, ambayo aliinyunyiza kila
upande wa mdhabahu. 19 Hata hivyo, waliyakata mafuta ya fahali na ya yule kondoo
dume, mafuta ya kwenye mkia, mafuta yafunikayo sehemu za ndani, figo, na yale
mafuta yaliyofunika mapafu. 20 Wakazichukua hizi sehemu zilizokatwa wakaziweka
juu ya vidari, na kisha Aroni akateketeza mafuta juu ya madhabahu. 21 Naye Aroni
akavitikisa vidari na paja la kulia kuwa sadaka ya kutikiswa mbele za Yahweh, kama
vile Musa alivyokuwa ameamru, 22 Kisha Aroni akainua juu mikono yake mbele ya
watu na kuwabariki, kisha akashuka chini kutoka mahali alipokuwa akitoa hiyo
sadaka ya dhambi, sadaka ya kuteketezwa, na sadaka ya amani. 23 Musa na Aroni
wakaingia ndani ya hema la kukutania, kisha wakatoka nje tena na kuwabariki
watu, na utukufu wa Yahweh ukaonekana kwa watu wote. 24 Moto ukashuka kutoka
kwa Yahweh na ukairamba sadaka ya kuteketezwa na mafuta yaliyokuwa juu ya
madhabahu. Watu wlipoona jambo hili, wakapiga kelele na kulala chini.

# 10

1 Nadabu na Abihu, wana wa Aroni, wakachukua kila mtu kifukizo chake, akaweka
moto ndani yake, na kisha uvumba. Kisha wakatoa moto usiokuabalika mbele
za Yahweh, moto ambao hakuwaamru wao kuutoa. 2 Kwa hiyo moto ukashuka
chini mbele za Yahweh na kuwala, nao wakafa mbele za Yahweh. 3 Kisha
Musa akamwambia Aroni, Hivi ndiyo Yahweh alivyokuwa akizunguzia aliposema,
'Nitaufunua utakatifu wangu kwa wale wajao mbele zangu. Nami nitatukuzwa mbele
za watu wote.'" Naye Aroni hakusema neno lolote. 4 Musa akamwita Mishaeli
na Elzafani, wana wa Uzieli mjomba wa Aroni, naye akamwambia, "njoo huku na
uwatowe ndugu zako nje ya kambi watoke mbele ya hema." 5 Hivyo wakakaribia
na kuwachukua wangali wamevaa kanzu zao za kikuhani, nao wakawapeleka nje
ya kambi, kama Musa alivyokuwa ameelekeza. Kisha Musa akamwambia Aroni
na wanawe wengine wawili, Eliezari na Ithamari, " 6 Msiache wazi nywele za
vichwa vyenu, wala msirarue nguo zenu, ili kwamba msije mkafa, na kwamba
Yahweh asilikasirikie kusanyiko zima. Lakini waacheni jamaa zenu, nyumba
yote ya Israeli waweze kufanya ibada za maombolezo kwa ajili ya hao ambao
Yahweh amewaangamiza kwa moto. 7 Msiende nje kutoka kwenye ingilio la hema
la kukutania, ama sivyo mtakufa, kwa kuwa mafuta ya Yahweh ya upako yako
juu yenu." Kwa hiyo wakatenda sawasawa na maelekezo ya Musa. 8 Mungu
akazungumza na Aroni, akisema, 9 "Msinywe mvinyo wala kinywaji kikali, wewe,
au wanao wanaobaki pamoja nawe, ili kwamba mtakapoingia kwenye hema ya
kukutania msije mkafa. Hii itakuwa amri ya kudumu katika vizazi vyote vya watu
wenu, 10 ili kupaambanua kati ya mambo matakatifu na mambo ya kawaida, na
kati ya najisi na safi, 11 ili kwamba mweze kuwafundisha watu wa Israeli amri
zote ambazo Yahweh ameziamru kwa kinywa cha Musa. 12 Musa akazungumza na
Aroni na wanawe wawili waliosalia; Eliazari naIthamari, Twaeni sadaka ya nafaka
inayobaki kutokana na sadaka ifanywayo kwa Yahweh kwa moto, nanyi ileni kando
ya madhabahu bila hamiara, kwa kuwa ni takatifu sana. 13 lazima mtaila mahali
patatifu kwa sababu huo ni mgao wako wewe na mgao wa wanao wa matoleo
yaliyofanywa kwa Yahweh kwa moto, kwa kuwa hivi ndivyo limeamriwa niwaambie.

14 Kile kidari kitikiswacho na lile paja ambalo hutolewa kwa Yahweh, yapasa mzile
mahali palipo safi panapokubalika kwa Mungu. Wewe mwenyewe, wanao na binti
zako waliopamoja nawe mtakula sehemu hizo, kwa kuwa zimetolewa kuwa mgao
wako na mgao wa wanao kutokana na dhabihu ya sadaka ya ushirika wa watu wa
Israeli. 15 Lile paja lililotolewa na kidari kilichotikiswa, ni lazima ziletwe pamoja
na sadaka ya mafuta iliyofanywa kwa moto, ili kutikiswa mbele za Yahweh. Nazo
zitakuwa zako wewe na wanao kuwa mgao wenu daima, kama Yahweh alivyoamru.
16 Kisha Musa akauliza kuhusu yule mbuzi wa sadaka ya dhambi, naye akagundua
kwamba alikuwa ametekezwa kwa moto. Kwa hiyo akawakasirikia Eliazari na
Ithamari, wana wa Aroni waliosalia; akawaambia, 17 “Kwa nini hamjaila sadaka ya
dhambi katika eneo la hema, kwa kuwa ni takatifu sana, na kwa kuwa Yahweh
amishaitoa kwenu ili kuchukua uovu wa kusanyiko, ili kufanya upatanisho kwa
aijli yao mbele zake? 18 Tazama, damu yake haikuletwa ndani ya hema, kwa hiyo
iliwapasa kwa hakika kuwa mekwisha ila kwenye eneo la hema, kama nilivyoagiza?
19 Kisha Aroni akamjibu Musa, “ Tazama, leo walitoa sadaka yao ya dhambi na sadaka
ya kuteketezwa mbele za Yahweh, na jambo hili vilevile limetendeka kwangu leo.
Ikiwa nimeshakula sadaka ya dhambi leo, Je! Isingekuwa imeshapendeza mbele za
Yahweh?” 20 Naye Musa aliposikia hivyo, akaridhika.

# 11

1 Yahweh akazungumza na Musa na Aroni, akasema, 2 “Sungumzeni na watu
wa Israeli muwaambie, 'Hivi ndivyo viumbe vyenye uhai ambavyo mwaweza kula
miongoni mwa wanyama walioko juu ya nchi. 3 Mnaweza kula mnyama yeyote
aliye na kwato zenye kugawanyika na ambaye pia hucheua. 4 Hata hivyo, kuna
baadhi ya wanyama ambao ama hawacheui au hana kwato zilizogawanyika, nanyi
msiwale hao, wanyama kama ngamia, kwa sababu yeye hucheua lakini hana kwato
zilizogawanyika. Kwa hiyo ngamia ni najisi kwenu. 5 Pimbi pia: kwa sababu yeye
hucheua lakini hana kwato zilizogawanyika mara mbili, huyo pia ni najisi kwenu.
6 Na sungura pia: kwa sababu yeye hucheua lakini hana kwato zilizogawanyika mara
mbili, huyu naye ni najisi kwenu. 7 Na nguruwe pia: ingawaje yeye anazo kwato
zilizogawanyika lakini hacheui, kwa hiyo yeye ni najisi kwenu. 8 Msile aina yoyote
ya nyama yao, wala msiiguse mizoga yao. Hao ni najisi kwenu. 9 Nao wanyama
waishio majini mnaoweza kuwala ni wale wote walio na mapezi na magamba,
iwe waliomo baharini au mitoni. 10 Lakini viumbe wote hai wasio na mapezi na
magamba waliomo baharini au mitoni, pamoja na wale waendao majini na viumbe
hai waliomo majini —watakuwa chukizo kwenu. 11 Kwa kuwa watakuwa chukizo,
msile nyama yao, pia mizoga yao sharti itakuwa chukizo. 12 Chochote kisichokuwa na
mapezi au magamba kilichomo majini ni lazima kiwe chukizo kwenu. 13 Nao ndege
mtakaowachukia na msiopaswa kuwala ni hawa wafuatao: tai, furukombe, kipungu,
14 mwewe mwekundu, aina yoyote ya kipanga, 15 kila aina ya kunguru, 16 kiruka-njia,
kipasuasanda, Shakwe, na aina yoyote ya mwewe. 17 Ni lazima pia bundi mdogo
na bundi mkubwa muwaone kuwa chukizo, mnandi, 18 bundi mweupe na mwari,
19 korongo na ina zote za koikoi, huduhudi na popo pia. 20 Wadudu wote wenye
mabawa wanatembea kwa miguu minne kwenu ni machukizo. 21 Lakini manaweza
kula wadudu wenye mabawa wanaotembea kwa miguu minne ya kurukia ardhini
yenye vifundo. 22 Na manaweza kula kula aina zote za nzige, senene, parare, au
panzi. 23 Lakini wadudu wote warukao wenye miguu minne ni chulkizo kwenu.
24 Nanyi mtakuwa najisi hata jioni kutokana na wanyama hawa endapo mtagusa
mizogo yao. 25 Na yeyote atakayeokota mojawapo wa mizoga yao ni lazima atazifua
ngua zake naye atakuwa najisi hata jioni. 26 Mnyama yeyote ambaye anazo kwato

ziliachana ambazo hazikugawanyika kabisa au hacheui huyo ni najisi kwenu. Yeyote
awagusaye atakuwa najisi. 27 Mnyama yeyote anayetembea kwa vitanga vyake
miongoni mwa wanyama waendao kwa miguu yote minne ni najisi kwenu. Yeyote
agusaye mzoga kama huo atakuwa najisi hata jioni. 28 Na yeyote aokotaye mzoga
kama huo ni zazima atazifua nguo zake na kuwa najisi hata jioni. Wanyama hawa
watakuwa najisi kwenu. 29 Kuhusiana na wanyama wataambaao juu ya ardhi, hawa
ndiyo walio najisi kwenu: kicheche, panya, aina zote za mijusi mikubwa, guruguru,
30 kenge, mijusi ya ukutani, goromoe, na kinyonga. 31 Wanyama hawa wote ambao
hutambaa, hawa ndiyo watakuwa najisi kwenu. Yeyote awagusaye atakuwa njisi
hata jioni. 32 Na iwapo mmoja wao anakufa na kuanguka juu ya chombo, chombo
hicho kitakuwa najisi, ama kiwe kimetengenezwa kwa mbao, nguo, ngozi, au gunia.
Kiwe chombo cha namna gani na kiwe kwa matumizi gani, ni lazima kitalowekwa
katika maji nacho kitakuwa najisi hata jio. Kisha kitakuwa safi. 33 Kwa hiyo kila
chungu ambacho mnyama najisi atakiangukia juu yake au ndani yake, chochote
kilichomo kwenye chungu hicho kitakuwa najisi, na ni lazima mtakivunja chungu
hicho. 34 Vyakula vyote ambavyo ni safi na kilichuhusiwa kuliwa, lakini kikaingiwa
na maji kutoka kwenye chungu najisi kilichoanguka, nacho kitakuwa najisi. 35 Na
kitu chochote kinachoweza kunywewa kutoka kwenye chungu kama hicho kitakuwa
najisi. Kila kitu kitakachoangukiwa juu yake na kipande cha mzoga wa mnyama
najisi nacho kitakuwa najisi, ama liwe ni jiko au vyungu vya kupikia. Ni najisi
na ni lazima kiwe najisi kwenu. 36 Chemchemi au kisima cha maji ya kunywa
yanapokusanyika patabaki kuwa safi iwapo kiumbe najisi kama hicho kitaangukia
humo. Lakini ikiwa yeyote anaugusa mzoga wa mnyama aliye najisi uliomo ndani
ya maji, yeye atakuwa najisi. 37 Iwapo sehehemu yoyote ya mzoga wa mnyama
aliyenajisi inaangukia juu ya mbegu zozote zilizo kwa ajili ya kupanda. Mbegu
hizo zitakuwa bado zingali safi. 38 Lakini kama maji yanawekwa juu ya mbegu, na
kama sehemu ya mzoga unaangukia juu yake, nazo zitakuwa najisi kwenu. 39 Iwapo
mnyama yeyote awezaye kuliwa anakufa, naye yeyote amgusaye atakuwa najisi hata
jioni. 40 Na yeyote alaye chochote cha mzoga huo atalazimika kufua nguo zake
naye atakuwa anjisi hata jioni. Na yeyote aokotaye mzoga kama huo atafua nguo
zake na kuwa najisi hata jioni. 41 Kila mnyama atambaaye juu ya ardhi atakuwa
chukizo; hatakuwa wa kuliwa. 42 Chochote kitambaacho kwa kujivuta juu ya tumbo
lake, na chochote kitembeacho kwa miguu yake yote minne, au chochote kilicho na
miguu mingi—wanyama wote ambao hutambaa juu ya nchi, hawa msiwale, kwa
sababu watakuwa machukizo. 43 Msijinajisi wenyewe kwa kiumbe chochote nnajisi
kitaambacho; msijinasi wenyewe kwavyo, ili kwamba msije mkachafuliwa navyo.
44 Kwa kuwa Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu. Nanyi lazima muwe watakatifu, kwa
hiyo na iweni watakatifu, kwa sababu Mimi ni mtakatifu. Haiwapasi kujichafua kwa
aina yoyote ya kiendacho juu ya nchi. 45 Kwa kuwa Mimi ndimi Yahweh, aliyewaleta
ninyi kutoka nchi ya Misri, ili niwe Mungu wenu. Kwa hiyo lazima muwe watakatifu,
kwa kuwa Mimi ni mtakatifu. 46 Hii ndiyo sheria kuhusu wanyama, ndege, kila
kiumbe hai kiendacho majini, na ya kila kiumbe kitambaacho juu ya nchi, 47 kwa
jili ya kilie kinachopaswa kutofautishwa kati ya kilicho najisi na kilicho safi, na kati
ya vitu vilivyokufa na vilivyo hai ambavyo vyaweza kuliwa na vitu vyenye uihai
visivyoweza kuliwa."

# 12

1 Yahweh akamwambia Musa, 2 "zungumza na watu wa Israeli, uwaambie, 'endapo
mwanamke anakuwa mjamzito na kujifungua mtoto wa kiume, naye atakuwa najisi
kwa muda wasiku saba, ni kama tu vile anavyokuwa najisi katika siku za kipindi

chake kwa mwezi. 3 Katika siku ya nane nyama ya govi la mtoto mvulana itatahiriwa.
4 Kisha utakaso wa mama wa kutokwa damu yake utaendelea kwa muda wa siku tatu.
Haimpasi kugusa kitu chochote kilicho kitakatifu au kukaribia eneo la hema mpaka
zitakapomalizika siku za kutakaswa kwake. 5 Lakini kama atajifungua mtoto wa kike,
naye atakuwa najisi kwa mud wa majuma mawili, kama alivyo wakati wa kipindi
chake. Kisha utakaso wa mama utaendelea kwa siku sitini sita. 6 Siku za kutakaswa
kwake zitakapoisha, kwa ajili ya mwana au binti, atalazimika kuleta kwa kuhani
mwana-kondoo wa mwaka mmoja kuwa sadaka ya kuteketezwa, na kinda la njiwa
au huwa kuwa sadaka ya dhambi, mbele ya ingilio la hema la kukutania, 7 Kisha
atawatoa mbele za Yahweh na kufanya sadaka ya upatanisho kwa ajili yake, naye
atatakaswa kutokana kutiririka kwa damu yake. Hii ndiyo sheria kuhusu mwanamke
aifunguaye ama mtoto wa kiume au wa kike. 8 Na kama hana uwezo wa kutoa
mwana-kondoo, naye ataleta makinda mawili ya njiwa ua hua, mmoja kwa ajili ya
sadaka ya kuteketezwa na mwingine kuwa sadaka ya dhambi, naye kuhani atafanya
upatanisho kwa ajili yake; naye atakuwa safi."

# 13

1 Yahweh akazungumza na Musa na Aroni, akasema, 2 Mtu yeyote anayeonekana
na uvimbe au pele au doa ling'aalo juu ya ngozi ya mwili wake, na likawa
limeambukizwa ugonjwa wa ngozi mwilini mwake, ni lazima aletwe kwa Aroni
kuhani mkuu au kwa mmoja wa wanawe makuhani. 3 Naye kuhanai atachunguza
ugonjwa huo kwenye ngozi ya mwili wake. Iwapo malaika zilizopo eneo lenye
ugonjwa zimegeuka kuwa nyeupe, na iwapo ugonjwa umejitokeza juu ya ngozi,
huo ni ugonjwa wa kuambukiza. Baada cha kuhani kumchunguza, atamtangaza
kuwa ni najisi. 4 Iwapo lile doa ling'aalo katika ngozi yake ni jeupe, na kuonekana
kwake halikwenda chini zaidi ya ngozi, na iwapo malaika za eneo lenye ugonjwa
hazijabadilika kuwa nyeupe, naye kuhani atamtenga mgonjwa kwa siku saba.
5 Katika siku ya saba, huyo kuhani itambidi kumchunguza tena ili kuona kama katika
maamzi yake huo ugonjwa siyo mbaya, na kama haujaenea kwenye ngozi. Iwapo
haujaenea, basi, kuhani atamtenga kwa siku saba zaidi. 6 Naye kuhani atamchunga
tena katika siku ya saba ili kuona kama ugonjwa ubepona na haujasambaa zaidi
kwenye ngozi. kama haujasambaa, basi, kuhani atamtangaza kuwa yeye ni safi.
Ni upele tu. Naye atafua nguo zake, na kisha yeye yu safi. 7 Lakini endapo ule
upele utakuwa umishasambaa kwenye ngozi baada ya kuwa amejionyesha kwa
kuhani kwa ajili kusafishwa kwake, itambidi kujionyesha tena kwa kuhani. 8 Naye
kuhani atamchunguza ilikuona kama huo upele umsambaa zaidi ndani ya ngozi.
Na endapo utakuwa umesambaa, kisha kuhani atamtangaza kuwa najisi. Huo ni
ugonjwa wa kuambukiza. 9 Iwapo ugonjwa wa ngozi wa kuambukiza umo kwa
mtu fulani, naye mtu huyo yapasa aletwe kwa kuhan. 10 Kuhani atamchunguza
ili kuona kama kunauvimbe mweupe katika ngozi yake, endapo malaika zitakuwa
zimebadilika kuwa nyeupe, au kumekuwa na nyama mbichi kwenye uvimbe. 11 Kama
ipo, basi, huo ni ugonjwa sugu wa ngozi, naye kuhani atamtangaza kuwa najisi.
Hatamtenga kwa kuwa yeye tayari ni najisi. 12 Iwapo huo ugonjwa unajitokeza
na kupanuka zaidi kwenye ngozi, na kuifunika ngozi ya mtu kwa ugonjwa tangu
kichwani pake hata miguuni, maadamu anajitokeza kwa kuhani, 13 naye kuhani
atamchunguza ili kuona kama huo ugonjwa umeshaenea mwili wake wote. Ikiwa
imetokeo hivyo, kuhani atamtangaza mtu huyo aliye na ugonjwa kuwa ni safi.
Ikiwa amebadilika kuwa mweupe, huyo ni safi. 14 Lakini ikiwa nyama mbichi
imeonekana juu yake, atakuwa najisi. 15 Kuhani ataiangalia hiyo nyama mbichi na
kumtanga kuwa najisi kwa sababu hiyo nyama mbichi ni najisi. Huo ni ugonjwa

wa kuambukiza. 16 Lakini endapo hiyo nyama mbichi inageuka kuwa nyeupe tena,
naye huyo mtu hana budi kwenda kwa kuhani. 17 Kuhani atamchunguza ili kuona
kama hiyo nyama imebadilika kuwa nyeupe. Kama imekuwa hivyo naye kuhani
atatangaza kwamba mtu huyo kuwa ni safi. 18 Mtu anapokuwa na jipu juu yangozi
yake na limishapona, 19 na mahali pa jipu pamekuwa na uvimbe au doa lenye kung'aa,
wekundu unaochanganyikana na weupe, yapasa kuonyeshwa kwa kuhani. 20 Naye
kuhani atalichunguza ili kuona kama linaonekana limekwenda chini ya ngozi, na
kama hizo malaika zimebadilika kuwa nyeupe, kama ni hivyo, kuhani atamtangaza
kuwa najisi. Huo ni ugonjwa wa kuambukiza, endapo utakuwa umezalishwa mahali
lilipokuwa jipu hilo. 21 Lakini endapo kuhani atakuwa amelichunguza na haoni
malaika nyeupe ndani yake, na kwamba iliko chini ya ngozi bali limefifia, kisha
kuhani atamtenga kwa siku saba. 22 Kama linaenea kwa kupanuka kwenye ngozi,
kisha kuhani atamtangaza kuwa najisi. Huo ni ugonjwa wa kuambukiza. 23 Lakini
kama hilo doa lenye kung'ara linabaki mahali pake na halijasambaa, basi hilo ni
kovu la jipu, naye kuhani atamtangaza kuwa safi. 24 Ngozi inapoungua na nyama
mbichi ya inamekuwa na wekundu uliochanganyika na weupe au doa jeupe, 25 kisha
kuhani ataichunguza kuona kama malaika zilizoko kwenye doa hilo zimebadilika na
kuwa nyeupe, na kama limeonekana kwenda chini zaidi ya ngozi, kama limekuwa
hivyo, basi huo ni ugonjwa wa kuambukiza. Umejitokeza kwenye jeraha la moto,
naye kuhani atamtangaza kuwa najisi. Huo ni ugonjwa wa kuambukiza. 26 Lakini
endapo kuahani analichunguza na naona kwamba hakuna malaika nyeupe kwenye
doa, na kwamba halikuenda chini ya ngozi bali linafifia, basi, kuhani atamtenga
mtu huyo kwa siku saba. 27 Kisha yapasa kuahani kumchunguza tena katika
siku ya saba. Iwapo litakuwa limesambaa kwa upana kwenye ngozi, naye kuhani
atamtangaza kuwa najisi. Huo ni ugojwa wa kuambukiza. 28 Iwapo hilo doa lisalia
mahali pake na halitakuwa limesambaa kwenye ngozi bali limefifia, ni uvimbe tu
kutokana na kuungua moto, naye kuhani atamtangaza kuwa safi, kwa kuwa siyo
zaidi ya jeraha la kuungua. 29 Iwapo mwanaume au mwanamke ana ugonjwa
wa kuambukiza kichwani au kidevuni pake, 30 kisha kuhani atamchunguza mtu
huyo kwa ajili ya ugonjwa wa kuambukiza ili kuona kama unakwenda ndani zaidi
ya ngozi, na kama kuna nywele za manjano, nyembamba ndani yake. endapo
zinaonekana, kisha kuhani atamtangaza kuwa najisi. Huo ni mwasho, ugonjwa
wa kuambukiza kichwani au kidevuni. 31 Iwapo kuhani anachunguza ugonjwa wa
mwasho na anagundu kuwa hauko chini ya ngozi, na kama hakuna nywele nyeusi
ndani yake, kisha kuhani atamtenga mtu huyo mwenye ugonjwa wa mwasho kwa
siku saba. 32 Katika siku ya saba kuhani atauchunguza tena huo ugonjwa ili kuona
kama umesambaa, Endapo hakuna malaika za manjano, na iwapo ugonjwa uko
usawa ngozi tu, 33 basi, yapasa mtu huyo kunyolewa., lakini sehemu yenye ugonjwa
haitanyolewa, naye kuhani atamtenga mtu huyo mwenye ugonjwa wa mwasho kwa
siku saba. 34 Katika siku ya saba kuhani atauchunguza tena ugonjwa ili kuona
kama umacha kusambaa ndani ya ngozi. Iwapo unaonekana kuwa hukwenda
chini zaidi ya ngozi, kisha kuhani atamtangaza kuwa safi. Mtu huyo yapasa kufua
nguo zake, na kisha atakuwa safi. 35 Lakini ikiwa ugonjwa wa mwasho umeenea
kwa sehemu kubwa kwenye ngozi baada ya kuhani kutangaza kuwa alikuwa safi,
36 naye kuhani itabidi amchunguze tena. Iwapo ugonjwa utakuwa umesambaa
katika ngozi, kuhani hahitajiki kutafuta nywele za manjano. Mtu huyo ni najisi.
37 Lakini iwapo katika mtazamo wa kuhani inaonekana kuwa huo ugonjwa wa
mwasho umekoma kusambaa, basi huo ugonjwa umekwisha pona. Yeye ni safi,
naye kuhani atamtangaza kuwa safi. 38 Iwapo mwanume au mwanamke ana madoa
juu ya ngozi, 39 kisha kuhani atamchunguza mtu huyo ili kuona kama hayo madoa

ni meupe kwa kufiifia, ambalo ni kovu tu lililojitokeza kwenye ngozi. Yeye yu
safi. 40 Iwapo nywele za mtu zimenyonyoka kichwani, yeye ni kipara lakini yu
safi. 41 Na iwapo nywele zake zimenyonyoka upande wa mbele wa kichwa chake,
na iwapo paji lake la uso lina kipara, yeye yu safi. 42 Lakini endapo kuna kidonda
chenye wekundu uliochanganyika na weupe, juu ya kipara chake au paji lake la
uso, huo ni ugonjwa wa kuambukiza uliojitokeza. 43 Naye kuhani atamchunguza ili
kuona iwapo uvimbe wa eneo linaugua juu ya upara wake au paji lake la uso lina
wekundu uliochanganyika na weupe, kama kuonekana kwa ugonjwa wa kuambukiza
kwenye ngozi. 44 Ikionekana hivyo, basi huyo ana ugonjwa wa kuambukiza naye
ni najisi. Hakika kuhani atamtangaza kuwa najisi kwa sababu ya ugonjwa wake
kichwani pake. 45 Mtu aliye na ugojwa wa kuambukiza atavaa nguo zilizochanika, ni
lazima nywele zake ziachwe wazi, na yampasa kufunika uso wake mpaka puani na
kupiga kelele, 'Najisi, najisi.' 46 Naye atakuwa najisi siku zote za ugonjwa wake wa
kuambukiza. Kwa sababu anao ugonjwa unaosambaa, yapasa kuishi peke yake nje
ya kambi. 47 Kuna wakati fulani vazi la mtu hupata ukungu juu yake. Laweza kuwa
vazi, ama la sufu au kitani, 48 au kitu chochote kilichosukwa au kufumwa kutokana
na sufu au kitani, au ngozi au kitu chochote kilichotengenezwa kwa ngozi. 49 Iwapo
sehemu iliyochafuliwa ina rangi ya kijani au nyekundu katika vazi, ngozi, kifaa
kilichosukwa au kufumwa, basi huo ni ukungu uanasambaa, ni lazima uonyeshwe
kwa kuhani. 50 Yapasa kuhani akichunguze hicho kifaa kwa ajili ya ukungu; ni lazima
akitenge kitu chochote kilicho na ukungu kwa siku saba. 51 Naye atauchunguza tena
huo ukungu katika siku ya saba. Endapo utakuwa umesambaa katika kifaa hicho,
basi ni wazi kwamba huo ni ukungu wenye kuangamiza, na hicho kifaa ni najisi.
52 Na mwenye kukimiliki atalazimika kukichoma na kukiteketeza kabisa hicho kifaa
kilichoonekana na ukungu ndani yake, haijalishi kiwe ni kifaa cha aina gani, kwani
huo ukungu unaweza kusababisha ugonjwa. 53 Iwapo kuhani anakichunguza hicho
kifaa na kuona kwamba ukungu haujaenea kwenye vazi au chombo kilichosukwa
au kusokotwa kutokana na sufu, kitani au ngozi, 54 basi atawaagiza wakisafishe
hicho kifaa kilichopatikana na ukungu, naye yampasa kukitenga kwa siku saba
zaidi. 55 Kisha kuhani atakichunguza tena hicho kifaa chenye ukungu baada ya kuwa
kimesafinshwa. Kama ukungu haukubadilika rangi yake, hata kama haukusambaa,
kifaa hicho ni najisi. Yapasa kichomwe, haijalishi ni wapi ukungu huo utakuwa
umekichafua. 56 Iwapo kuhani anakichunguza hicho kifaa, na kama ukungu umefifia
baada ya kuwa umeoshwa, basi atakirarua kile kipande kilichochaufuliwa kutoka
kwenye vazi au kutoka kwenye ngozi, au kutoka kwenye chombo kilichosukwa au
kusokotwa. 57 Ikiwa ukungu unazidi kuonekana katika vazi, ama katika chombo
kilichosukwa au kufumwa, au katika kitu chochote kilichotengenezwa kwa ngozi,
basi, ukungu utakuwa unasambaa. Kifaa chochote kilicho na ukungu ni lazima
kichomwe. 58 Vazi au kitu chochote kilichosukwa au kufumwa kutokana na sufu, au
kitani, au ngozi au kitu chochote kilichotengenezwa kwa ngozi—iwapo unakisafisha
kifaa nao ukungu ukawa umetoka, nacho kifaa lazima kisafishwe mara ya pili, kisha
kitakuwa safi. 59 Hii ndiyo sheria ihusuyo ukungu katika vazi la sufu au kitani, au
kwenye kitu chochote kilichosukwa au kufumwa kutokana na sufu, au kitani, au kitu
chochote kilichotengenewa kwa ngozi, ili kwamba mweze kuvitangaza kuwa safi au
najisi.

## 14

1 Yahwe alizungumza na Musa, akisema, 2 “Hii itakuwa sheria kwaajili ya mtu
aliyekufa kwenye siku ya utakaso. Lazima aletwe kwa kuhani. 3 Kuhani atakwenda
nje ya kambi kumchunguza mtu kuona kama madhara ya ugonjwa wa ngozi

yameponywa. 4 Ndipo kuhani ataamuru kwamba mtu mwenye kutakaswa lazima
achukue ndege safi wawili, waliohai, mti wa mwerezi, kitani nyekundu na hisopo.
5 Kuhani atamwamuru kuua moja ya hao ndege juu ya maji safi yaliyo kwenye chungu
cha udongo. 6 Ndipo kuhani atamchukua ndege aliyehai na mti wa mwerezi, na kitani
nyekundu na hisopo, na vyote hivi, pamoja na ndege aliyehai atavichovya kwenye
damu ya ndege aliyechinjiwa kwenye maji safi. 7 Ndipo kuhani atanyunyiza maji haya
mara saba juu ya mtu anayetakaswa katika ugonjwa, na ndipo kuhani atamtangaza
kuwa msafi. Ndipo kuhani atamwachia ndege aliyehai katika eneo wazi. 8 Mtu
aliyetakaswa atafua nguo zake, atanyoa nywele zake zote, ataoga kwa maji, na ndipo
atakuwa safi. Baada ya hayo lazima aje kwenye kambi, lakini ataishi nje ya hema lake
kwa siku saba. 9 Katika siku ya saba lazima anyoe nywele za kichwa chake, na lazima
pia anyoe ndevu zake na nyusi. Lazima anyoe nywele zake zote, na lazima afue
nguo zake na aoge kwenye maji; ndipo atakuwa safi. 10 Katika siku ya nane lazima
achukue dume wa wana kondoo wawili wasio na lawama, mwana kondoo jike wa
mwaka mmoja asiye na lawama, na tatu ya kumi ya efa ya unga safi uliochanganywa
mafuta kama sadaka ya nafaka, na kipimo kimoja cha mafuta. 11 Kuhani ambaye
amemtakasa mtu atamsimamisha mtu ambaye aliyemtakasa, pamoja na vile vitu,
mbele ya Yahwe mahali pa kuingilia kwenye hema ya mkutano. 12 Kuhani atachukua
mmoja wa wanakondoo dume na kumtoa kama sadaka ya hatia, pamoja na kipimo
cha mafuta; atavitikisa kwa sadaka ya kutikiswa mbele ya Yahwe. 13 Lazima aue
mwana kondoo dume mahali ambapo wanapochinjia sadaka ya dhambi na sadaka
ya kuteketezwa, katika eneo la hema, sababu sadaka ya dhambi ni ya kuhani, kama
afanyavyo sadaka ya hatia, kwasababu ni takatifu zaidi. 14 Kuhani atachukua baadhi
ya damu ya sadaka ya hatia na kuiweka kwenye ncha ya sikio la kulia la mtu yule wa
kutakaswa, katika dole gumba la kulia, katika dole la mguu wa kulia. 15 Ndipo kuhani
atachukua mafuta kutoka chombo na kuyamimina katika kiganja cha mkono wake
wa kushoto, na kuzamisha kidole chake katika mafuta hayo yaliyo kwenye mkono
wa kushoto, 16 na kunyunyiza baadhi ya mafuta kwa kidole mara saba mbele za
Yahwe. 17 kuhani ataweka mafuta yaliyobaki kwenye mkono wake kwenye ncha ya
sikio la kulia la mtu wa kutakaswa, juu ya dole gumba la mkono wa kulia, na katika
dole kubwa la mguu wa kulia. Lazima aweke mafuta haya juu ya damu kutoka
kwenye sadaka ya hatia. 18 Kama kwa mafuta yaliyosalia kwamba katika mkono wa
kuhani, atayaweka juu ya kichwa cha mtu ambaye atakaswaye, na kuhani atafanya
utakaso kwaajili yake mbele za Yahwe. 19 Ndipo kuhani atatoa sadaka ya dhambi na
kufanya upatanisho kwaajili yake atakaswaye kwa sababu ya kutokuwa safi kwake,
na badaye ataua sadaka ya kuchomwa. 20 Ndipo kuhani atatoa sadaka ya kuteketezwa
na sadaka ya nafaka juu ya madhabahu. Kuhani atafanya upatanisho kwaajili ya mtu
huyo, na ndipo atakuwa safi. 21 Kwa namna hiyo, kama mtu ni masikini na hawezi
kumudu matoleo haya, ndipo anaweza kuchukua kondoo mmoja dume kama sadaka
ya hatia ya kutikiswa, kufanya upatanisho kwaajili yake mwenyewe, na moja ya
kumi ya efa ya unga safi uliochanganywa na mafuta kama sadaka ya nafaka, na
chombo cha mafuta, 22 pamoja na njiwa wawili au kinda mbili za njiwa, ambao
anaweza kupata; ndege mmoja atakuwa sadaka ya dhambi na mwingine sadaka
ya kuteketezwa. 23 Katika siku ya nane lazima awalete kwa kuhani kwaajili ya
utakaso, pakuigilia katika hema ya mkutano, mbele ya Yahwe. 24 Kuhani atachukua
mwana kondoo kwaajili ya sadaka, na atachukua pamoja na kiasi cha mafuta ya
mzeituni, na ataviinua juu kama anaviwasilisha kwa Yahwe. 25 Atamuua mwana
kondoo kwaajili ya sadaka ya hatia, na atachukua baadhi ya ya damu ya sadaka ya
hatia na kuiweka juu ya ncha ya sikio la kulia la yule wakutakaswa, juu ya dole
gumba la mkono wake wa kulia, na kwenye dole kubwa la mguu, wa kulia. 26 Ndipo

kuhani atamimina baadhi ya mafuta katika kiganja cha mkono wake wa kushoto,
27 na atanyunyiza kwa kidole chake cha kulia baadhi ya mafuta ambayo yako kwenye
mkono wa kushoto mara saba mbele za Yahwe. 28 Ndipo kuhani ataweka kiasi cha
mafuta ambayo yako kwenye mkono wake kwenye ncha ya sikio la yule mtu wa
kutakaswa, katika dole gumba lake la mkono wa kulia, na dole kubwa la mguu wa
kulia, maeneo yale yale ambayo kaweka damu ya sadaka ya hatia. 29 Ataweka mafuta
yaliyobaki yaliyo mkononi mwake juu ya yule wakutakaswa, kufanya upatanisho
kwaajili yake mbele za Yahwe. 30 Lazima atoe sadaka ya njiwa au makinda ya njiwa,
yale ambayo mtu ameweza kupata - 31 moja kama ya sadaka ya dhambi na nyingine
kama sadaka ya kuteketezwa, pamoja na sadaka ya nafaka. Ndipo kuhani atafanya
upatanisho kwaajili ya yule ambaye atatakaswa mbele za Yahwe. 32 Hii ni sheria
kwaajili ya mtu kwake kuna athari za ugonjwa wa ngozi, ambaye hawezi kumudu
kiwango cha sadaka kwaajili ya utakaso wake." 33 Yahwe alizungumza na Musa
na Haruni, akisema, 34 "Wakati mtakuja katika nchi ya Kanaani ambayo nimewapa
kama miliki, na kama naweka ukungu unaenea ndani ya nyumba katika nchi ya
miliki yenu, 35 ndipo yeye ambaye anamiliki nyumba ile lazima aje na kumwambia
kuhani. Lazima aseme 'Inaonekana kwangu kuna kitu fulani kama ukungu ndani
ya nyumba yangu.'" 36 Ndipo kuhani ataamuru kwamba watoe vitu vyote ndani
kabla hajaenda ndani kuona uthibitisho wa ukungu, kiasi kwamba hakuna ndani ya
nyumba kitakachofanywa najisi. Badaye kuhani lazima aende ndani kuona humo
ndani. 37 Yeye lazima achunguze ukungu kuona kama umo katika kuta za nyumba,
na kuona ikiwa kunaonekana ukijani au wekundu katika bonde za mwonekano
wa kuta. 38 Kama nyumba inao ukungu, ndipo kuhani atatoka nje ya nyuma na
kufunga mlango wa nyumba kwa siku saba. 39 Ndipo kuhani atarudi tena katika
siku ya saba na kuichunguza kuona kama ukungu umeenea katika kuta za nyumba.
40 Kama hivyo, ndipo kuhani ataamuru kwamba wayaondoe mawe ambayo ukungu
umepatikana na yatupwe katika sehemu najisi nje ya mji. 41 Yeye atataka kuta zote
za ndani ya nyumba zikwanguliwe, na lazima achukue vitu vilivyochafuliwa na
hivyo vilivyokwanguliwa nje ya mji na kuvitupa kwenye eneo lisilosafi. 42 Lazima
wayachukue mawe mengine na kuyaweka katika sehemu ya mawe yaliyoondolewa,
na lazima watumie udongo mpya kupigia lipu nyumba. 43 Kama ukungu unakuja tena
na unaingia katika nyumba ambayo mawe yameondolewa na kuta zimekwanguliwa
na kupigwa lipu upya, 44 ndipo kuhani lazima aje aingie ndani na kuchunguza
nyumba kuona kama ukungu umeenea ndani ya nyumba. Kama hivyo, huo ni
ukungu mbaya, na nyumba ni najisi. 45 Nyumba hiyo lazima iangushwe chini. Hayo
mawe, mbao, na lipu yote ndani ya nyumba lazima vibebwe kupelekwa nje ya mji
kwenye sehemu najisi. 46 Kwa nyongeza, yeyote anaenda ndani ya nyumba wakati
imefungwa atakuwa najisi mpaka jioni. 47 Na yeyote aliyelala ndani ya nyumba
lazima afue nguo zake, na yeyote aliyekula ndani ya nyumba lazima afue nguo
zake. 48 Kama kuhani akaingia hiyo kuichunguza kuona ikiwa ukungu umeenea
katika nyumba baada ya nyumba kupigwa lipu, ndipo, kama ukungu umetoweka,
ataitangaza nyumba hiyo kuwa ni safi. 49 Ndipo kuhani lazima achukue ndege wawili
kuitakasa nyumba, na mti wa mwelezi, na sufu nyekundu, na hisopo. 50 Atamuua
ndege mmojawapo katika maji masafi kwenye dumu la udongo. 51 Atachukua mti wa
mwerezi, hisopo, sufu nyekundu na ndege aliyehai, na kuvichovya kwenye damu ya
ndege aliyekufa, kwenye maji safi, na kunyunyizia nyumba mara saba. 52 Ataitakasa
nyumba kwa damu ya ndege na maji safi, pamoja na ndege aliyehai, mti wa mwerezi,
hisopo, na sufu nyekundu. Lakini atamwachia ndege aliyehai aende nje ya mji
mashambani. 53 Kwa njia hii lazima afanye upatanisho kwaajili ya nyumba, na
itakuwa safi. 54 Hii ni sheria kwa aina zote za athari ya ugonjwa wa ngozi na vitu

vyote vinavyosababisha ugonjwa kama huo, na kwaajili ya kuwashwa, [55] na kwa
ukungu kwenye mavazi na nyumba, [56] kwaajili ya uvimbe, kwaajili ya vipele, madoa,
[57] kutambua wakati wowote tatizo hili ni najisi au lini limetakaswa. Hii ni sheria
kwaajili ya athari za ugonjwa wa ukungu.

# 15

[1] Yahwe alizungumza na Musa na Haruni, akisema, [2] "Waambie watu wa Israeli, na
sema kwao, 'Wakati mtu yeyote kisonono kimemwathiri mwili wake unatoa ugiligili,
anakuwa najisi. [3] Unajisi wake unatokana na athari ya kisonono. Iwe mwili wake
unatoa ugiligili au umekoma, huo ni unajisi." [4] Kitanda chochote anachokilalia
kitakuwa najisi, na kila kitu ambacho anakaa juu yake kitakuwa najisi. [5] Yeyote
anayegusa kitanda chake lazima afue nguo zake na aoge kwenye maji, na awe
amenajisika mpaka jioni. [6] Yeyote anayekaa katika kitu chochote ambacho mtu
ambaye ameathiriwa na kisonono alikaa, mtu huyo lazima afue nguo zake na aoge
katika maji, na atakuwa najisi mpaka jioni. [7] Na yeyote anayegusa mwili wa ambaye
ameathirika na kisonono lazima afue nguo zake na aoge katika maji, na awe najisi
hadi jioni. [8] Kama mtu ambaye anaona majimaji kama hayo kwa mtu fulani ambaye
ametakasika, ndipo mtu huyo lazima afue nguo zake na aoge kwenye maji, na
atakuwa najisi hata jioni. [9] Tandiko lolote ambalo ambaye anamajimaji ya kisonono
atalikalia litakuwa najisi. [10] Yeyote anayegusa kitu chochote kilichokuwa chini ya
mtu huyo atakuwa najisi mpaka jioni, na yeyote anayebeba vitu hivyo lazima afue
nguo zake na aoge katika maji; atanajisika mpaka jioni. [11] Ambaye anamajimaji
kama hayo akimgusa kabla kwanza ya kuosha kwa maji safi mikono yake, mtu
aliyeguswa lazima afue nguo zake na aoge katika maji, na atakuwa najisi mpaka
jioni. [12] Chungu chochote cha udongo ambacho ambaye anamajimaji kama hayo
akigusa lazima kivunjwe, na kila chombo cha mti lazima kioshwe na maji safi.
[13] Wakati mwenye kisonono anapotakaswa katika kisonono chake, ndipo lazima
ahesabu kwaajili yake siku saba kwaajili ya kutakasika kwake; ndipo afue nguo
na aoshe mwili wake kwenye maji yatiririkayo. Ndipo atakuwa safi. [14] Katika
siku ya nane lazima achukue njiwa wawili au kinda mbili za njiwa na aje mbele
za Yahwe pakuingilia kwenye hema ya mkutano; pale lazima atoe hao ndege kwa
kuhani. [15] Lazima kuhani awatoe, moja kama sadaka ya dhambi na nyingine kama
ya kuteketezwa, na kuhani lazima afanye upatanisho kwaajili yake mbele za Yahwe
kwaajili ya kisonono chake. [16] Kama mtu yeyote ametokwa na shahawa, ndipo lazima
aoge mwili wake wote katika maji; atanajisika mpaka jioni. [17] Kila vazi au ngozi
ambayo juu yake kuna shahawa lazama paoshwe kwa maji; itakuwa najisi mpaka
jioni. [18] Na kama mwanamke na mwanaume watalala pamoja na kunakutokwa kwa
shahawa kwenda kwa mwanamke, lazima wote wawili waoge katika maji; watakuwa
najisi mpaka jioni. [19] Mwanamke anapokuwa kwenye hedhi, ataendelea kunajisika
kwa siku saba, na yeyote anayemgusa atakuwa najisi mpaka jioni. [20] Chochote
anacholala juu yake wakati wa hedhi kitakuwa najisi; kila kitu ambacho anakalia
kitakuwa pia najisi. [21] Yeyote anayegusa kitanda chake lazima afue nguo zake na
aoge kwa maji; mtu huyo atakuwa najisi mpaka jioni. [22] Yeyote anayegusa chochote
ambacho amekikalia lazima afue nguo zake na aoge kwa maji; mtu huyo anakuwa
najisi mpaka jioni. [23] Iwe juu ya kitanda au kitu chochote juu ya popote atakapokaa,
kama akikigusa, mtu huyo atakuwa najisi mpaka jioni. [24] Kama mwanaume yeyote
akilala naye, na unajisi wa mwanamke ukamgusa, atakuwa amenajisika siku saba.
Kila kitanda ambacho anakilalia mwanaume huyo kitanajisika. [25] Kama mwanamke
ametokwa damu kwa siku nyingi ambayo siyo kipindi cha hedhi yake, au ikitoka
zaidi ya kipindi chake cha hedhi, wakati wote wa siku za kunajisika, atakuwa kama

alikuwa kwenye siku zake za hedhi. Yeye ni najisi. 26 Kila kitanda anachokilalia
wakati wote wa kutokwa damu itakuwa kwake sawa tu kama kitanda anacholalia
wakati wa hedhi, na kila kitu ambacho anakalia kitakuwa najisi, kama tu unajisi wa
hedhi yake. 27 Na yeyote anayegusa kitu kati ya vitu hivyo atakuwa najisi; lazima
yeye afue nguo zake na aoge mwenyewe kwenye maji, na atakuwa amenajisika
mpaka jioni. 28 Lakini kama mwanamke ametakasika katika kutokwa na damu, ndipo
atahesabu kwaajili yake siku saba, baada ya hizo atakuwa safi. 29 Katika siku ya nane
atachukua kwake njiwa wawili au kinda wawili wa njiwa na atawaleta kwa kuhani
pakuingilia hema ya mkutano. 30 Huyo kuhani atatoa ndege mmoja kama sadaka ya
dhambi na mwingine kama sadaka ya kuteketezwa, na atafanya upatanisho kwaajili
ya huyo mbele ya Yahwe kwaajili unajisi wa mwanamke atokwaye damu. 31 Hivi
ndivyo lazima uwatenge watu wa Israeli katika unajisi wao, hivyo hawatakufa tokana
na unajisi wao, kwa kuchafua hema langu, ambapo naishi kati yao. 32 Huu ndio
utaratibu kwa kila ambaye anakisonono, kwaajili kila mwanaume ambaye shahawa
yake inatoka na inamfanya kuwa najisi, 33 kwaajili ya mwanamke ambaye yuko
katika kipindi cha hedhi, kwaajili ya yeyote aliye na kisonono, awe mwanaume au
mwanamke, na kwaajili ya yeyote anayelala na mwanamke najisi.

# 16

1 Yahwe alizungumza na Musa - hii ni baada vifo vya wana wawili wa Haruni,
walipomkaribia Yahwe na ndipo wakafa. 2 Yahwe alimwambia Musa, “Ongea na
Haruni kaka yako na umwambie hapana kuja tu wakati wowote katika patakatifu pa
patakatifu ndani ya pazia, mbele ya kifuniko cha upatanisho kilicho juu ya sanduku.
Akifanya hivyo, anakufa, kwasababu naonekana katika wingu juu ya kifuniko cha
upatanisho. 3 Hivi ndivyo jinsi Haruni lazima aje katika patakatifu pa patakatifu.
Yeye lazima aingie pamoja na ndama kama sadaka ya dhambi, na kondoo dume
kama sadaka ya dhambi. 4 Ni lazima avae kanzu ya kitatani, na lazima avae ndani
yake nguo ya kitani, na lazima avae mshipi wa kitani na kilemba cha kitani. Haya
ni mavazi matakatifu. Lazima aoge mwili wake katika maji na avae mavazi haya.
5 Lazima achukue kwenye umati wa watu wa Israeli mbuzi wawili waume kama
sadaka ya dhambi na kondoo dume moja ikiwa ni sadaka ya kuteketezwa. 6 Ndipo
Haruni lazima alete ng'ombe kama sadaka ya dhambi, ambayo itakuwa kwaajili yake
mwenyewe, kufanya upatanisho kwaajili yake mwenyewe na familia yake. 7 Ndipo
lazima achukue mbuzi wawili na kuwaweka mbele ya Yahwe katika mlango wa
kuingilia kwenye hema ya mkutano. 8 Ndipo Haruni lazima apige kura kwaajili
ya mbuzi hao wawili, kura moja kwaajili ya Yahwe, na kura nyingine kwaajili ya
msingiziwa. 9 Ndipo Haruni lazima awasilishe mbuzi ambaye kura imeangukia kwa
Yahwe, na kumtoa mbuzi huyo kama sadaka ya dhambi. 10 Lakini mbuzi ambaye
kura ya usingiziwa imemwangukia lazima aletwe kwa Yahwe akiwa hai, kufanya
upatanisho kwa kumwachia aende porini kama, mbuzimsingiziwa. 11 Pia Haruni
lazima alete ng'ombe kwaajili ya sadaka ya dhambi, ambayo itakuwa kwaajili yake
mwenyewe, lazima afanye upatanisho kwaajili yake mwenyewe na familia yake,
hivyo lazima yeye amuue huyo ng'ombe kama sadaka ya dhambi kwaajili yake
mwenyewe. 12 Haruni lazima achukue chetezo iliyojaa mkaa wa moto kutoka kwenye
madhabahu mbele ya Yahwe, na mikono imejaa ubani mzuri, na kuleta vitu hivi
ndani ya pazia. 13 Hapo lazima aweke ubani juu ya moto mbele za Yahwe ili
kwamba wingu kutoka kwenye ubani liweze kufunika kifuniko cha agano la imani
ya upatanisho. Yeye afanye hivyo ili kwamba asife. 14 Ndipo lazima achukue kiasi
cha damu ya ng'ombe na kuinyunyiza kwa kidole chake mbele ya kifuniko cha
upatanisho. Lazima anyunyize kiasi cha damu kwa kidole chake mara saba mbele ya

kifuniko cha upatanisho. 15 Ndipo lazima aue mbuzi kwaajili ya sadaka ya dhambi
ambayo ni kwaajili ya watu na kuileta damu yake ndani kwenye pazi. Hapo lazima
aifanyie damu kama alivyofanya kwenye damu ya fahali: lazima ainyunyize juu
ya kifuniko cha upatanisho na mbele ya kifunuko cha upatanisho. 16 Yeye lazima
afanye upatanisho kwaajili ya mahali patakatifu kwa sababu ya matendo ya unajisi
ya watu wa Israeli, na kwa sababu ya uasi na dhambi zao zote. Yeye pia lazima
afanye haya kwaajili ya hema ya mkutano, ambapo Yahwe anaishi kati yao, katika
uwepo wa matendo yao ya unajisi. 17 Hakuna mtu anayetakiwa kuwepo katika hema
ya mkutano wakati Haruni anaingia kufanya upatanisho katika mahali patakatifu
pa patakatifu, na mpaka atoke nje na amemaliza kufanya upatanisho kwaajili yake
mwenyewe na kwaajili ya familia yake, na kwaajili umati wa Israeli. 18 Yeye lazima
aende nje kwenye madhabahu hapo mbele za Yahwe na kufanya upatanisho kwaajili
ya hiyo, na lazima achukue kiasi cha damu ya mbuzi na kuiweka juu ya pembe za
madhabahu yote kuzunguka. 19 Anatakiwa anyunyize kiasi cha damu juu yake kwa
kidole chake mara saba kuitakasa na kuitenga maalumu kwa Yahwe, mbali kutoka
matendo ya unajisi wa watu wa Israeli. 20 Atakapo maliza kupatanisha kwaajili
ya mahali patakatifu sana, hema la mkutano, na madhabahu, lazima amlete mbuzi
aliyehai. 21 Haruni lazima aweke mikono yake yote juu ya kichwa cha mbuzi huyu
aliyehai na akiri juu yake maovu yote ya watu wa Israeli, uasi wao wote, dhambi zao
zote. Ndipo lazima aweke dhambi hizo juu ya kichwa cha mbuzi na amwachie katika
uangalizi wa mtu aliyetari kumwongoza mbuzi huyo porini. 22 Mbuzi lazima abebe
juu yake mwenyewe uovu wote kwenda mahali pakiwa. Kule msituni, huyo mtu
amwache mbuzi aende huru. 23 Ndipo Haruni anapaswa kwenda tena humo kwenye
hema ya mkutano na kuvua mavazi ya kitani ambayo amayavaa kabla hajaenda
mahali patakatifu sana, na anatakiwa kuyaacha mavazi hayo pale. 24 Anapaswa
aoshe mwili wake kwa maji mahali patakatifu, na avae nguo zake za kawaida; pia
lazima atoke nje kutoa sadaka ya kuteketezwa na sadaka ya kuteketezwa na sadaka
ya kuteketezwa kwaajili ya wale watu, na kwa njia hii anafanya upatanisho kwaajili
yake mwenyewe na kwaajili ya watu. 25 Lazima yeye achome mafuta ya sadaka ya
dhambi juu ya madhabahu. 26 Huyu mtu anayemwacha mbuzi msingiziwa aende
huru anafua nguo zake na kuosha mwili wake katika maji; baada ya hayo, anaweza
kurudi tena kambini. 27 Yule fahali kwaajili ya sadaka ya dhambi na mbuzi kwaajili
ya sadaka za dhambi, ambaye damu yake ililetwa kufanya upatanisho katika mahali
patakatifu, lazima ipelekwe nje ya kambi. kule lazima wachome, ngozi zao, nyama
yao na kinyesi chao. 28 Huyu anayechoma sehemu hizo lazima afue nguo zake na
aoge mwili wake katika maji; baada ya hapo, anaweza kurudi tena kwenye kambi.
29 Hii itakuwa sharti kwaajili yenu kwamba katika mwezi wa saba, kwenye siku
ya kumi ya mwezi, mtanyenyekea wenyewe na msifanye kazi, iwe mwenyeji wa
kuzaliwa au mgeni anayeishi kati yenu. 30 Hii ni kwasababu katika siku hii ya
upatanisho utafanywa kwaajili yenu, kuwatakasa ninyi kutoka dhambi zenu zote
ili mwe safi mbele za Yahwe. 31 Hii ni maalumu kwa Sabato ya kupumzika kwaajili
yenu, na lazima mnyenyekee wenyewe na msifanye kazi. Hili litakuwa sharti kati
yenu. 32 Kuhani mkuu, ambaye atapakwa mafuta na kuwekwa wakfu kuwa kuhani
mkuu katika nafasi ya baba yake, lazima afanye upatanisho huu na kuvaa mavazi
ya kitani, hayo ni mavazi matakatifu. 33 Lazima afanye upatanisho kwaajili ya
mahali patakatifu sana; lazima afanye upatanisho kwaajili ya hema ya mkutano
na madhabahu, na lazima afanye upatanisho kwaajili ya makuhani na kwaajili ya
kusanyiko la watu. 34 Hii daima itakuwa sharti kwaajili yako, kufanya upatanisho
kwaajili ya watu wa Israeli kwasababu ya dhambi zao zote, mara moja kwa kila
mwaka." Na ilikuwa ikifanika kama Yahwe alivyomwamuru Musa.

# 17

1 Yahweh akamwambia Musa, 2 “Zungumza na Aroni na wanawe, na watu wote wa
Israeli. Waambie mambo ambayo ameamru Yahweh: 3 Mtu yeyote wa Isreli anayeua
fahali au mwana—kondoo au mbuzi kambini, au amuuaye nje ya kambi, ili kumtoa
dhabihu— 4 kama hamleti katika ingilio la hema la kukutania ili kumtoa dhabihu kwa
Yahweh mbele za hema lake la kukutania, mtu huyo ana hatia ya damu iliyomwagika.
Amemwaga damu, na mtu huyo ni sharti akatiliwe mabali kutoka miongoni mwa
watu wake. 5 Kusudi la amri hii ni kwamba watu wa Israeli wataleta dhabihu zao kwa
Yahweh kwenye ingilio la hema la kukutania, watazileta kwa kuhani ziweze kutolewa
kuwa matoleo ya shukrani kwa Yahweh, badala ya kutoa dhabihu hadharani katika
shamba. 6 Kuhani atainyunyiza damu juu ya madhabahu ya Yahweh kwenye ingilio la
hema la kukutania; atayachoma mafuta yake ili kutoa harufu ya kupendeza mbele za
Yahweh. 7 Ni lazima watu wasitoe tena dhabihu zao kwa sanamu za mbuzi, ambazo
kwazo hutenda kama makahaba. Hili litakuwa agizo la kudumu kwa ajili yao katika
vizazi vya watu wao vyote. 8 Ni lazima uwaambie, 'Mtu yeyote wa Israeli, au Mgeni
yeyote aishiye miongoni mwao, atoweye dhabihu 9 na asiilete kwenye ingilio la hema
la kukutania ili kuitoa kwa Yahweh, mtu huyo ni lazima akatiliwe mbali kutoka kwa
watu wake.' 10 Na Mtu yeyote wa Israeli, au yeyote wa Wageni anayeishi miongoni
mwao, ambaye hunywa damu; nitamkatilia mbali atoke miongoni mwa watu wake.
11 Kwa kuwa uhai wa mnyama yeyote umo katika damu yake. Nimeitoa damu yake
kwenu kufanya upatanisho juu ya madhabahu kwa ajili ya uhai wenu, kwa sababu
ni damu ndiyo ifanyayo upatanisho, kwa kuwa ni damu ipatanishayo kwa ajili ya
uhai 12 Kwa hiyo Niliwaambia Watu wa Israeli kwamba hayupo miongoni mwenu
impasaye kula damu, wala yeyote wa Wageni aishiye miongoni mwenu atakaye kula
damu. 13 Na yeyote miongoni mwa watu wa Israeli, au yeyote wa Wageni aishiye
miongoni mwenu ni lazima aimwage damu ya mnyama na kuifukia hiyo damu kwa
mafumbi. 14 Kwa kuwa uhai wa kila kiumbe umo katika damu yake. Ni kwa sababu
hii niliwaambia watu wa Israeli, ni lazima msile damu ya kiumbe cho chote, kwa
kuwa maisha ya kila kiumbe chenye uhai ni damu yake. Yeyeote ailaye ni lazima
akatiliwe mbali. 15 Mtu yeyote alaye mnyama aliyekufa au ambaye amelaruliwa na
wanyama pori, ama yule mtu ni mwenyeji wa kuzaliwa au ni mgeni aishiye miongoni
mwenu, ni lazima atazifua nguo zake na kujiosha katika maji, naye atakuwa najisi
hata jioni. Kisha atakuwa safi. 16 Lakini kama hazifui nguo zake au kuosha mwili
wake, ni lazima aichukue hatia yake”.

# 18

1 Yahweh akazungumza na Musa, akisema, 2 “Zungumza na watu wa Israeli na
uwaambie, “Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu. 3 Msitende mambo ambayo watu
wa Misri huyatenda, mahali mlikokuwa mkiishi awali. Na ni lazima msitende
mambo yale wanayoyatenda watu wa Kanaani, nchi ambayo ninawapeleka nyinyi.
Msifuate desturi zao. 4 Sheria zangu ndizo mtakazozitenda, na amri zangu ndizo
mtakazozishika, kwa sababu Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu. 5 Kwa hiyo ni lazima
mzitunze hukumu zangu na sheria zangu. Ikiwa mtu amezitii, ataishi kwa sababu
ya hizo. Mimi Ndimi Yahweh. 6 Pasiwepo kwenu atakayelala na yeyote aliye na
uhusiano wa karibu naye. Mimi ndimi Yahweh. 7 Usimfedheheshe baba yako kwa
kulala na mama yako. Yeye ni mama yako! Haikupasi kumfedhehesha yeye. 8 Usilale
na yeyote wa wake za baba yako; Usimfedheheshe namna hiyo baba yako. 9 Usilale
na yeyote aliye mmoja miongoni mwa dada zako, ama ni binti ya baba yako au ni
binti ya mama yako, ama aliyelelewa nyumbani mwenu au mbali nawe. Usilale na
dada zako. 10 Usilale na binti ya mwanao, au binti ya binti yako. Hiyo ingekuwa

aibu yako mwenyewe. [11] Usilale na binti ya mke wa baba yako, aliyezaliwa kwa
baba yako, yeye ni dada yako, na usilale naye. [12] Usilale na dada ya baba yako.
Yeye ni ndugu wa karibu kwa baba yako. [13] Usilale na dada ya mama yako. Yeye ni
ndugu wa mama yako. [14] Usimfedheheshe ndug wa baba yako kwa kulala na mke
wake. Usimkaribie kwa kusudi hilo; yeye ni shangazi yako. [15] Usilale na binti- mkwe
wako, Yeye ni mke wa mwanao; usilale naye. [16] Usilale na mke wa kaka yako; usije
ukamfedhesha yeye katika njia hii. [17] Usilale na mwanamke kisha na binti yake, au
binti wa mwanawe au binti wa binti yake. Hao ni ndugu zake wa karibu, na kulala
nao lingekuwa ni uovu. [18] Usimwoe dada ya mke wako kuwa mke wako wa pili na
kulala naye wakati bado mke wako wa kwanza angali hai. [19] Usilale na mwanamke
wakati wake wa hedhi. [20] Yeye ni najisi kwa wakati huo. Usilale na mke wa jilani
yako na kujichafua mwenyewe kwake katika njia hii. [21] Msiwatoe watoto wenu ili
kuwapitisha kwenye moto, ili kwamba muwatoe sadaka kwa Moleki, kwa sababu
msije mkalinajisi jina la Mungu wenu. Mimi ndimi Yahweh. [22] Usilale na mwanaume
mwingine kama ulalavyo na mwanamke. Jambo hili lingekuwa uovu. [23] Usilale na
myama yeyote na kujitia unajisi kwake. Haimpasi mwanamke kufikiria kulala na
mnyama ye yote. Huo ungekuwa upotovu. [24] Msijichafue wenyewe katika njia hizi,
kwa kuwa katika njia hizi mataifa yamechafuliwa, mataifa ambayo Nitayafukuza
yatoke kwa ajili yenu. [25] Ni kwa sababu nchi imenajisiwa, hivyo niliiadhibu dhambi
yao, nayo nchi ikawatapika wakazi wake [26] Kwa hiyo, yawapasa kuzishika amri
zangu na maagiza yangu, na msifanye aina yoyote ya mambo haya ya machukizo,
wala Mwisraeli mzaliwa au Mgeni aishie miongoni mwenu. [27] Kwa kuwa ni uovu
huu ambao watu wametenda, wale ambao waliishi hapa kabla yenu, na sasa nchi
imenajisiwa. [28] Kwa hiyo, muwe waangalifu ili kwamba nchi isiwatapike nyinyi
baada ya kuwa mmeinajisi, kama ilivyowatapika wale watu waliokuwako kabla
yenu. [29] Yeyote anayefanya mambo haya ya kuchukiza, watu wafanyao mambo
hayo ya kuchukiza lazima watakatiliwa mbali kutoka miongoni mwa watu wao.
[30] Kw a hiyo inawapasa kuzishika amri zangu na sitende mojawapo ya desturi hizi
zenyekuchukiza ambazo zilitendwa hapo kabla yenu, ili msijinajisi wenyewe kwa
hizo. Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu.

# 19

[1] Yahweh akazungumza na Musa, akisema. [2] Zungumza na kusanyiko lote la watu
wa Israeli na uwaambie, 'Ni lazima muwe watakatifu, kwa kuwa mimi Yahweh
Mungu wenu ni mtakatifu. [3] Kila mtu amstahi mama yake na baba yake. Na ni
lazima muzishike Sabato zangu. Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu. [4] Msizigeukie
sanamu zisizo na thamani, wala kujitengenezea wenyewe miungu kutokana na
chuma. Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu. [5] Unapotoa dhabihu za sadaka ya ushirika
kwa Yahweh, utatoa ili kupata kibali. [6] Ni sharti iliwe siku hiyo hiyo uliyoitoa, au siku
inayofuata. [7] Kama kinabaki kitu cho chote hata siku ya tatu ni lazima kiteketezwe
kwa moto. Kama kitaliwa katika siku ya tatu kitakuwa najisi. Hakitakubalika,
[8] lakini kila akilaye ni lazima atachukua hatia yake kwa sababu amekivunjia heshima
kilicho kitakatifu kwa Yahweh. Mtu huyo ni lazima akatiliwe mbali na watu wake.
[9] Unapovuna mavuno ya ardhi yako, usivune hata pembezo mwa shamba lako kabisa,
wala hutakusanya mabaki ya mavuno yako yote. [10] Usikusanye kila zabibu kutoka
katika mizabibu yako, wala usiziokote dhabibu zilizoanguka chini katika shamba la
mizabibu. Ni lazima uziache kwa ajili ya masikini na kwa ajili ya wageni. Mimi
ndimi Yahweh Mungu wako. [11] Usiibe. Usiseme uongo. Msidanganyane. [12] Usiape
kwa jina langu kwa uongo na kulinajisi jina la Mungu wako. Mimi ndimi Yahweh
[13] Usimgandamize jirani yako wala kumwibia. Usishikilie malipo ya kibarua usiku

kucha hata asubuhi. 14 Usimlaani kiziwi au kuweka kikwazo mbele ya kipofu. Badala
yake, yakupasa umwogope Mungu wako. Mimi ndimi Yahweh. 15 Usisababishe
hukumu ikawa ya uongo. Usionyeshe upendeleo kwa mtu fulani eti kwa kuwa tu yeye
ni masikini na usionyeshe upendeleo kwa mtu fulani eti kwa kuwa tu yeye ni mtu
muhimu. Badala yake, amua juu ya jirani yako kwa haki. 16 Usiende huku na huko
ukisema habari za uchochezi miongoni mwa watu wako, bali tafuta kuyalinda maisha
ya jirani yako. Mimi ndimi Yahweh. 17 Usimchukie ndugu yako moyoni mwako.
Mkemee jirani yako kwa heshima ili kwamba usishiriki katika dhambi kwa sababu
yake. 18 Usijilipize kisasi au kuwa na chuki yoyote dhidi ya mtu yeyote wa watu wako,
lakini badala yake mpende jirani yako kama unavyojipenda wewe mwenyewe. Mimi
ndimi Yahweh. 19 Shika amri zangu. Usiwazalishe wanyama wako kwa kutumia
wanyama wa aina nyingine tofauti. Usichanganye aina mbili tofauti za mbegu
unapopanda shamba lako. Usivae vazi lililofumwa kwa kutumia nyuzi za rangi
mbili tofauti zilizochanganywa pamoja. 20 Yeyote anayelala na msichana mtumwa
aliyeposwa na mume mwingine, lakini ambaye hajakombolewa au hajaachwa huru,
lazima waadhibiwe. Hawatauawa kwa sababu yule msichana hakuwa huru. 21 Ni
lazima mtu huyo alete sadaka yake ya hatia kwenye ingilio la hema la kukutania—
kondoo dume iwe sadaka ya hatia. 22 Kisha kuhani atafanya upatanisho kwa ajili
yake kwa huyo kandoo dume mbele za Yahweh kutokana na dhambi aliyoitenda.
Nayo dhambi iliyotendwa itasamehewa. 23 Mtakapoingia katika nchi na kupanda
aina zote za miti kwa chakula, kisha mtayahesabu matunda yatakayozaliwa kuwa
yamekatazwa kuliwa. Tunda litakatazwa kwako kwa miaka mitatu. Halitaliwa.
24 Lakini katika mwaka wa nne matunda yote yatakuwa matakatiifu, matoleo ya sifa
kwa Yahweh. 25 Katika mwaka wa tano unaweza kula tunda, ambalo umelisubiri ili
kwamba mti uweze kuzaa zaidi. Mimi ndimi Yahweh Mungu wako. 26 Usile nyama
yoyote amabayo damu ingalimo ndani yake. Usiulize kwa roho juu ya wakati ujao,
27 Usitafute kuwadhibiti wengine kwa njia ya nguvu za kichawi. Msifuate tabia za
kipagani kama vile kunyoa denge au kunyoa pembe za ndevu zeu. 28 Usiukate mwili
wako kwa ajili ya wafu au kuchanja chale juu ya mwili wako. Mimi ndimi Yahweh.
29 Usimwaibishe binti yako kwa kumfanya kahaba, la sivyo taifa litaangukia kwenye
ukahaba na nchi itajawa na uovu. 30 Utazitunza Sabato zangu na kupaheshimu
mahali patakatifu pa hema langu la kukutania. Mimi ndimi Yahweh. 31 Msiwageukie
wale wanaoongea na wafu au roho wachafu. msiwatafute, la sivyo watawanajisi
ninyi, Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu. 32 Ni lazima usimame mbele za mtu
mwenye mvi na uheshimu uwepo wa mzee. Yakupasa umwegope Mungu wako. Mimi
ndimi Yahweh. 33 Mgeni anapoishi miongoni mwenu katika nchi yanu, usimtendee
lolote lililobaya. 34 Mgeni anayeishi pamoja nanyi ni lazima awe kama mwenyeji
Mwisraeli mzaliwa anayeishi kwenu, na sharti umpende kama unavyojipenda wewe
mwenyewe, ni kwa sababu wewe ulikuwa mgeni katika nchi ya Misri. Mimi ndimi
Yahweh Mungu wako. 35 Unapopima urefu, uzito, au wingi usitumie vipimo vya
udanganyifu. 36 Tumia mizani iliyo halali, mawe ya kupimia uzito yaliyo halali, efa
halali, hini iliyo halali. Mimi ndimi Yahweh Mungu wako, aliyekutoa katika nchi ya
utumwa ya Misri. 37 Utayatii maagizo yangu na sheria zangu zote na kuzitenda. Mimi
ndimi Yahweh.

# 20

1 Yahweh akazungumza na Musa, akasema, 2 “Waambie watu wa Waisraeli, 'mtu
yeyote miongoni mwa watu Israeli, au Mgeni yeyote anayeishi miongoni mwa
Waisraeli atakayemtoa mtoto wake yeyote kwa Moleki, hakika atauawa. Ni lazima
watu wa nchi wamponde kwa mawe. 3 Pia nitaukaza uso wangu dhidi ya mtu

huyo na kumkatilia mbali kutoka miongoni mwa watu wake kwa sababu amemtoa
mtoto wake kwa Moleki, ili kupatia unajisi mahali pangu patakatifu na kulinajisi
jina langu takatifu. 4 Na kama watu wa nchi watayafumba macho yao kwa mtu
huyo anapomtoa mmoja wa watoto wake kwa Moleki, kama hawatamwua mtu
huyo, ndipo Mimi mwenyewe nitaukaza uso wangu dhidi ya mtu huyo na ukoo
wake, 5 Nami nitamkatilia mbali pamoja na yeyote anayejifanya kahaba ili kufanya
umalaya na Moleki. 6 Mtu yule anayewageukia wanaozungumza na wafu, au na wale
wanaozungumza na roho ili kufanya ukahaba nao, Nitakaza uso wangu dhidi ya mtu
huyo; Nami nitamkatilia mbali atoke miongoni mwa watu wake. 7 Kwa hiyo jitakaseni
wenyewe na muwe watakatifu, kwa sababu Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu.
8 Mtazitunza amari zangu na kuzifuta. Mimi ndimi Yahweh anayewatenga ninyi
muwe watakatifu. 9 Yeyote amlaaniye baba yake au mama yake hakika mtu huyo
atauawa. Amemlaani baba yake au mama yake, kwa hiyo ana hatia na anastahili
kufa. 10 Mwanaume yeyote afanyaye uzinzi na mke wa mwanaume mwingine, yaani,
yeyote anayezini na mke wa jirani yake—yule mwanaume mzinzi na mwanamke
mzinzi ni lazima wote wawili wauawe. 11 Mwanaume yeyote anayelala na mke
wa baba yake ili kukutana naye kimwili amemfedhehesha baba yake mwenye.
Wote wawili; mwana huyo na mke huyo wa baba yake kwa hakika watauawa.
wanahatia na wanastahili kufa. 12 Kama mwanaume atalala na mke wa mwanawe,
wote wawili; mwanaume huyo na mke huyo wa mwanawe hakika watauawa.
Wametenda upotovu. Wana hatia na wanastahili kufa. 13 Kama mwanaume analala
na mwanaume mwingine kama alalavyo na mwanamke, wote wawili watakuwa
wamefanya jambo lililo ovu. Hakika watauawa. Wana hatia na wanastahili kufa.
14 Ikiwa mwanaume atamwoa mwanamke na pia akamwoa mama wa mwanamke
huyo, huu ni uovu. Ni lazima wachomwe kwa moto, wote wawili, mwanaume huyo
na manamke huyo, ili kwamba hapatakuwepo na uovu miongoni mwenu. 15 Ikiwa
mwanaume analala na mnyama, hakika atauawa, ni lazima mumuue na mnyama
huyo pia. 16 Ikiwa mwanamke anamkaribia mnyama ili kulala naye, ni lazima
mmuuwe mwanamke huyo pamoja na mnyama. Kwa hakika ni lazima wauawe.
wana hatia na wanastahili kufa. 17 Ikiwa mwanaume analala na dada yake, ama
ni binti ya baba yake au binti ya mama yake—ikiwa wamelala pamoja, hilo ni
jambo la aibu. Ni lazima wakatiliwe mbali watoke machoni pa watu wao, kwa
sababu amelala na dada yake. Ni lazima aibebe hatia yake. 18 Kama mwanaume
analala na mwanamke katika kipindi cha hedhi yake, na amekutana naye kimwili,
atakuwa amefunua mtiririko wa damu yake, chanzo cha damu yake. Ni lizima
wote wawili wakatiliwe mbali kutoka mingoni mwa watu wao. 19 Usilale na dada
ya mama yako, au dada ya baba yako, kwa sababu ungeweza kumwaibisha jamaa
yako wa karibu. Ni lazima utabeba hatia yako mwenyewe. 20 Ikiwa mwanaume
analala na shangazi yake, atakuwa amemfedhehesha mjomba wake. Wanapokufa,
nitawaadhibu wote wawili, na wanapokufa nitauondolea mbali urithi wa watoto
wao ambao wangeliupokea kutoka kwa wazazi wao. 21 Ikiwa mwanaume anamwoa
mke wa kaka yake wakati ambapo kaka yake angali hai, hilo ni jambo la aibu.
Amemfedhehesha kaka yake, na nitaondolea mbali mali yoyote amabayo watoto
wao wangerithi kutoka kwa wazazi wao. 22 Kwa hiyo imewapasa kuzishika amri na
sheria zangu zote; ni lazima mzitii ili kwamba ile nchi ambayo ninawaleta kuishi
isiwatapike nyinyi. 23 Msienende katika desturi za mataifa ambayo nitayafukuza
mbele yenu, ni kwa sababu wamefanya mambo haya yote, nami mimewachukia wao.
24 Nami nikawaambia ninyi, “Mtaimiliki nchi yao, nitaitoa kwenu ili muimiliki, nchi
itiririkayo amaziwa na asali. Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu, aliyewatenga nyinyi
kutoka kwa watu wengine. 25 Ni lazima pia mtofautishe kati ya wanya najisi na

wale walio safi, na kati ya ndege walio najisi na walio safi. Msijichafue wenyewe
kwa wanyama au ndege au kiumbe kitambaacho juu ya nchi kilicho najisi, ambacho
nimekitenga kuwa najisi. [26] Mtakuwa watakatifu, kwa kuwa Mimi, Yahweh, ni
mtakakatifu, nami nimewatenga nyinyi kutoka kwa watu wengine, kwa kuwa nyinyi
ni wangu. [27] Mwanaume au mwanamke anayeongea na wafu au anayeongea na roho
hakika atauawa. Watu watawaponda kwa mawe. Wanayo hatia na wanastahili kufa.

# 21

[1] Yahweh akamwambia Musa, “Zungumza na makuhani, wana wa Aroni, nawe
waambie, 'hakuna hata mmoja miongoni mwenu atakayejitia unajisi kwa wale
wanaokufa miongoni mwa watu wake, [2] isipokuwa yule aliye ndugu wa karibu—
mama yake, baba yake, mwanawe, bintiye, nduguye, [3] au dada yake bikira
anayemtegemea, kwa kuwa hana mume—kwake huyo anaweza kujitia unajisi.
[4] Lakini hatajitia unajisi na kujichafu kwa ajili ya jamaa wengine. [5] Makuhanai
hawatanyoa vichwa vyo wala kunyoa pembeni mwa ndevu zao, wala hawatachanja
chale miili yao. [6] Watakuwa watakatifu kwa Mungu wao, wala hawataliaibisha jina
la Mungu wao, kwa sababu makuhani hutoa sadaka ya Yahweh ya chakula, mkate wa
Mungu wao. Kwa hiyo makuhani lazima wawe watakatifu. [7] Hawataoa mwanamke
aliye kahaba na aliyetiwa unajisi, na hawataoa mwanamke aliyetalikiwa kutoka kwa
mume wake kwa sababu wametengwa kwa ajili ya Mungu wao. [8] Utamtenga kwa
sababu yeye ndiye anayetoa mkate kwa Mungu wako. Ni lazima awe mtakatifu,
kwa sababu—Mimi, Yahweh, ndimi niwatakasaye nyinyi—pia Mimi mwenyewe
ni mtakatifu. [9] Binti yeyote wa kuhani anayejitia unajisi kwa kujifanya kahaba
anajifedhehesha mwenyewe. Ni lazima ateketezwe kwa moto. [10] Mtu ambaye
ni kuhani mkuu miongoni mwa nduguze, ambaye mafuta ya upako yamekwisha
kumiminwa kichwani pake, na ambaye amekwisha kuwekwa wakfu ili kuvaa mavazi
maalum ya kuhani mkuu, kamwe hataziacha wazi nywele zake wala hatazirarua
nguo zake. [11] Hataingia kamwe mahali popote ambapo kuna maiti na kujitia unajisi,
hata kama ni maiti ya baba yake au ya mama yake. [12] Kuhani mkuu hataondoka
eneo takatifu la hema la kukutania au kupatia unajisi patakatifu pa Mungu wake,
kwa sababu amewekwa wakfu kuwa kuhani mkuu kwa kutiwa mafuta ya upako ya
Mungu wake. Mimi ndimi Yahweh. [13] Kuhani mkuu nilazima aoe bikira kuwa mke
wake. [14] Hataoa mjene, mwanamke mtalaka au mwanamke aliye kahaba. Anaweza
kuoa mwanamke bikira kutoka kwa watu wake, [15] kwa hiyo asiwatia unajisi watoto
wake miongoni mwa watu wake. kwa kuwa Mimi Yahweh, ndimi ninayemfanya
yeye mtakatifu.” [16] Yahweh akamwambia Musa, akasema, [17] Zungumza na Aroni na
umwambie, 'mtu yeyote wa ukoo wako katika vizazi vyako vyote mwenye kasoro
mwilini mwake, asisogee kutoa chakula kwa Mungu wake. [18] Mtu yeyote mwenye
kasoro mwilini mwake asimkaribie Yahweh, [19] mtu kama vile: kipofu au mtu
asiyeweza kutembea, mtu aliyeharibiwa uso au kupungukiwa na viungo mwilini, mtu
aliye na mguu au mkono wenye ulemavu, [20] mtu mwenye kibiongo mgongoni mwake
au aliye na kimo kidogo au wembamba usio wa kawaida, au mtu mwenye kasoro
machoni mwake, au mwenye ugonjwa, kidonda, upele, au yule ambaye korodani
zake zimeharibiwa. [21] Hakutakuwa na mtu miongoni mwa ukoo wa Aroni kuhani
mkuu mwenye kasoro mwilini atakayekaribia kutoa matoleo yatakayoteketezwa kwa
moto kwa ajili ya Yahweh. Mtu kama huyo mwenye kasoro mwilini hatakaribia ili
kutoa mkate wa Mungu wake. [22] Anaweza kula chakula cha Mungu wake, ama iwe
baadhi ya vile vilivyo vitakatifu sana au vile vitakatifu. [23] Hata hivyo, hataingia
ndani ya pazia wala kuisogelea madhabahu, kwa sababu ana kasoro mwilini mwake,
ili kwamba asipanajisi mahali patakatifu pangu, kwa kuwa Mimi ndimi Yahweh

anayewafanya watakatifu.” [24] Kwa hiyo Musa akamwambia maneno haya Aroni,
wanawe, na watu wote wa Israeli.

## 22

[1] Yahweh akazungumza na Musa, kusema, [2] “Ongea na Aroni na wanawe,
waambie wajiepushe na vitu vitakatifu vya watu wa Israeli wanavyovitenga kwangu.
Wasilinajisi jina langu. Mimi ndimi Yahweh. [3] Waambie, 'Ikiwa mmoja wa wazao
wenu katika vizazi vyenu vyote anakaribia vitu vitakatiifu vile ambavyo watu wa
Israeli wamevitenga kwa Yahweh, wakati akiwa najisi, sharti mtu huyo akatiliwe
mbali atoke mbele zangu. Mimi ndimi Yahweh. [4] Hatakuwapo yeyote wa uzao
wa Aroni aliye na ungonjwa wa ngozi wa kuambukiza, au maambukizi yatirirkayo
kutoka mwilini mwake, atakayekula sehemu yoyote ya dhabihu inatolewayo kwa
Yahweh mpaka atakapotakasika. Yeyote agusaye kitu chochote kilichonajisi kwa njia
ya kugusa maiti, au kwa kumgusa mtu yeyote aliyetokwa na shahawa, [5] au yeyote
agusaye mnyama atakayemtia unajisi, au mtu yeyote atakayemfanya najisi, kwa hiyo
unajisi wowote unaweza kuwa— [6] kuhani yeyote agusaye kitu chochote kisichosafi
atakuwa najisi hata jioni. Hatakula chochote cha vitu vitakatifu, isipokuwa ameuosha
mwili wake katika maji. [7] Jua linapotua, ndipo atakuwa safi. Baada ya machweo
anaweza kula kutoka katika vitu vitakatifu, kwasababu hivyo ni vyakuala vyake.
[8] Asile mzoga wowote uliookotwa au mnyama aliyeraruliwa na wanyama pori,
ambaye kwake atajitia unajisi. Mimi ndimi Yahweh. [9] Ni lazima makuhani wafuate
maagizo yangu, ama sivyo watakuwa na hatia ya dhambi na wangeweza kufa kwa
kunitia unajisi. Mimi ndimi Yahweh ninayewafanya wao watakatifu. [10] Hakuna mtu
kutoka nje ya familia ya kuahani, wakiwemo wageni wa kuhani au watumwa wake
wa kuajiliwa, atakayeweza kula kitu chochote kilicho kitakatifu. [11] Lakini kama huyo
kuhani amenunua mtumwa kwa fedha yake mwenyewe, mtumwa huyo anaweza
kula kutoka katika vitu vilivyotengwa kwa Yahweh. Na watu wa familia ya kuhani
na watumwa waliozaliwa nyumbani mwake, pia wanaweza kula pamoja naye kutoka
katika vitu hivyo. [12] Ikiwa binti wa kuhani ameolewa na mtu asiye kuhani, hataweza
kula chochote cha mchango wa matoleo matakatifu. [13] Lakini ikiwa huyo binti wa
kuhani ni mjane au ametalikiwa, na ikiwa hana mtoto, na anarudi kuishi knyumbani
kwa baba yake kama alivyokuwa wakati wa ujana wake, anaweza kula kutoka
katika chakula cha baba yake. Lakini hakuna yeyote asiye wa familia ya kikuhani
anatakayeruhusiwa kula kutoka katika chakula cha kuhani. [14] Kama mtu anakula
chakula kitakatifu bila ya kukijua, naye atamlipa kuahani kwa ajili ya hicho; itampasa
kuongeza moja ya tano juu yake na kukirejesha kwa kuhani. [15] Haiwapasi watu
wa Israeli kutoheshimu vitu vitakatifu ambavyo vimeinuliwa juu na kuletwa kwa
Yahweh, [16] kisha wakajisababishia wenyewe kuchukua dhambi amabyo ingewafanya
kuwa na hatia ya kula chakula kitakatifu, kwa kuwa mimi ndimi Yahweh awafanyaye
wao watakatifu.” [17] Yahweh akazungumza na Musa, akasema, [18] “Sema na Aroni
na wanawe, na kwa watu wa Israeli wote. Waambie, Mwisraeli yeyote, au Mgeni
anayeishi katika Israeli, waletapo dhabihu—iwe ni kutimiza kiapo, au iwe ni sadaka
ya hiari, au wanaleta kwa Yahweh sadaka ya kuteketezwa kwa moto, [19] ikiwa
wanataka ikubalike, ni lazima watowe mnyama dume asiye na dosari, kutoka kwenye
kundi la ng'ombe, kondoo au mbuzi [20] Lakini hamtatoa chochote kilicho na dosari.
Sitakipokea kwa niaba yenu. [21] Yeyote atoae dhabihu ya sadaka ya ushirika kutoka
katika kundi la ng'ombe au la kondoo kwa Yahweh ili kutimiza kiapo, au kama
sadaka ya hiari, ili ikubalike, ni lazima isiwe na kilema. Ni lazima pasiweko na
kasoro katika mnyama. [22] Msitoe kabisa wanyama waliovipofu, waliojeruhiwa,
wala walio na kilema, wenye upele, vidonda vitokavyo usaha, wala wenye vigaga.

Msiwatoe hawa kuwa dhabihu ya kuteketezwa kwa moto iliyotolewa kwa Yahweh
juu ya madhabahu. 23 Unaweza kumleta makisai au mwana-kondoo mlemavu au
aliyedumaa kuwa sadaka ya hiari, lakini sadaka kama hiyo kwa ajili kutimiza kiapo,
haitapokelewa. 24 Usitoe kwa Yahweh mnyama yeyote aliyetiwa jeraha, kupondwa,
au kukatwa korodani zake. 25 Usifanye haya katika nchi yako. Usilete mkate wa
Mungu wako kutoka mkononi mwa mgeni. Hao wanyama wenye vilema na dosari
ndani yao, hawatapokelewa kabisa kwa ajili yako. 26 Yahweh akamwambia Musa na
akasema, 27 “Wakati ndama, mwana—kondo au mwana—mbuzi azaliwapo, sharti
abaki na mama yake kwa muda wa siku saba. Ndipo kuanzia siku ya nane na
kuendelea, anaweza kupokelewa kuwa dhabihu iliyofanywa kwa moto kwa Yahweh.
28 Usimchinje ng'ombe jike pamoja na ndama wake au mbuzi jike pamoja na kitoto
chake kwa siku moja. 29 Utoapo sadaka ya shukrani kwa Yahweh utaitoa kwa njia
iliyokubalika. 30 Ni lazima iliwe siku iyo hiyo inayotolewa. Hutakiwi kubakiza
chochote hata asubuhi. Mimi ndimi Yahweh. 31 Kwa hiyo imewapasa kuzishika amri
zangu na kuzifuata. Mimi ndimi Yahweh. 32 Msiliabishe jina langu takatifu. Ni lazima
nitambuliwe kuwa ni mtakatifu na watu wa Israeli. Mimi ndimi Yahweh niwafanyaye
ninyi watakatifu, 33 ambaye amewaleta kutoka katika nchi ya Misri ili niwe Mungu
wenu: Mimi ndimi Yahweh.”

# 23

1 Yahweh akamwambia Musa: 2 “Zungumza na watu wa Israeli, na uwaambie,
'Hizi ndizo sikukuu zilizoamriwa kwa ajili ya Yahweh, ambazo ni lazima mzitangaze
kuwa makusanyiko matakatifu, ni sikukuu zangu za mara kwa mara. 3 Mnaweza
kufanya kazi kwa siku sita, lakini siku ya saba ni Sabato ya kupumzika kabisa.
Usifanye kazi kwa sababu ni Sabato kwa ajili ya Yahweh mahali pote mnaposhi. 4 Hizi
ndizo sikukuu za Yahweh zilizoamriwa, Makusanyiko matakatifu mtakayoyatangaza
kwa nyakati zilioamriwa: 5 Katika mwenzi wa kwanza, siku ya kumi na nne ya
mwezi kwenye mwanga hafifu wa machweo ya jua, ni Pasaka ya Yahweh. 6 Siku
ya kumi na tano ya mwezi ule ule ni sikukuu ya mikate isiotiwa hamira kwa ajili
ya Yahweh. Kwa muda wa siku saba mtakula mikate isiotiwa hamira. 7 Siku ya
kwanza ni lazima mjitenge kwa pamoja, hamtafanya kazi ya kawaida. 8 Kwa siku
saba mtamletea Yahweh matoleo ya chakula. Siku ya saba ni ya kusanyiko takatifu
lililotengwa kwa ajili ya Yahweh, nanyi katika siku hiyo hamtafanya kazi yoyote
ya kawaida.” 9 Yahweh akamwambia Musa, akisema, 10 “Sema na watu wa Israeli
uwaambie, 'mtakapika kwenye nchi nitakayowapa nyinyi, na mtakapovuna mazao
yake, nanyi yawapasa kumletea kuhani fungu la masuke ya nafaka ya matunda
yake ya kwanza. 11 Naye ataliinua hilo fungu la masuke ya nafaka mbele za
Yahweh na kulileta kwake, kwa kuwa litakubalika kwa niaba yenu. Nalo litaletwa
siku baada ya Sabato ili kwamba kuhani ataliinua na kulileta kwangu. 12 Siku
ile mtakapoliinua lile fungu la masuke ya nafaka na kulileta kwangu, itawabidi
kutoa mwana—kondoo dume wa mwaka mmoja na asiye na dosari awe sadaka
ya kuteketezwa kwa Yahweh. 13 Matoleo ya nafaka yatakuwa sehemu za kumi za
efa za unga laini uliochanganywa na mafuta, uwe matoleo yaliyofanywa kwa moto
kwa Yahweh, ili kutoa harufu nzuri ya kupendeza, pamoja na hiyo kutakuwa na
matoleo ya kinywaji ya divai, moja ya nne ya hini. 14 Hamtakula mkate, wala
nafaka iliyokaangwa au nafaka mpya hata siku ile mliyoleta matoleo haya kwa
Mungu wenu. Hii itakuwa amri ya kudumu katika vizazi vyote vya watu wenu,
popote pale mnapoishi. 15 Tangu siku iliyofuata baada ya Sabato—hiyo ilikuwa
siku mlipolileta lie fungu la nafaka la matoleo ya kutikiswa—hesabuni majuma
saba kamili. 16 Mtahesabu siku hamsini, ambazo zingekuwa siku baada ya Sabato

ya saba. Kisha mtaleta matoleo ya nafaka mpya kwa Yahweh. 17 Mtaleta kutoka
nyumbani mwenu mikate miwili iliyotengenezwa kutokana na mbili za kumi za efa.
Ni lazima ifanywe kwa unga laini na uliochanganywa na hamira; zitakuwa matoleo
ya kutikiswa ya malimbuko ya kwanza kwa Yahweh. 18 Mtaileta hiyo mikate pamoja
na wana—kondoo saba wa mwaka mmoja na wasiokuwa na dosari, fahali mmoja
mchanga na dume wa kondoo wawili. Watakuwa matoleo ya kuteketezwa kwa moto
kwa Yahweh, pamoja na matoleo yao ya nafaka na matoleo ya kinywaji, matoleo
yaliyofanywa kwa moto na kutoa harufu nzuri ya kupendeza kwa Yahweh. 19 Ni
lazima mtowe mbuzi dume mmoja kwa ajili ya matoleo ya dhambi, na wana—kondoo
dume wawili wa mwaka mmoja kwa ajili ya dhabihu, wawe matoleo ya ushirika.
20 Ni lazima kuhani azitikise pamoja na mkate wa malimbuko ya kwanza mbele za
Yahweh na kuzileta kwake kuwa matoleo pamoja na kondoo dume wawili. Watakuwa
sadaka takatifu kwa Yahweh kwa ajili ya kuhani. 21 Mtatoa tangazo siku iyo hiyo.
Kutakuwa na kusanyiko takatifu, na hamtafanya kazi za kawaida. Hii itakuwa amri
ya kudumu katika vizazi vya watu wenu mahali pote mnapoishi. 22 Mtakapovuna
mazao ya nchi yenu, Msivune kabisa kabisa pembeni mwa mashamba yenu, wala
msivune mazazo ya mavuno yenu. Inawapasa kuyaacha kwa ajili ya masikini na
mgeni. Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu." 23 Yahweh akazungumza na Musa,
akisema, 24 "Zungumza na watu wa Israeli na uwaambie, "Siku ya kwanza ya mwezi
wa kwanza itakuwa siku ya pumzika makini kwa ajili yenu, kumbukumbu pamoja
na kupigwa kwa tarumbeta na kusanyiko takatifu, 25 Hamtafanya kazi ya kawaida,
na ni lazima mtoe dhabihu inayofanywa kwa moto kwa Yahweh." 26 Kisha Yahweh
akamwambia Musa, akisema, 27 "Sasa, siku ya kumi ya mwezi huu wa saba, ni Siku ya
Upatanisho. Kutakuwa na kusanyiko takatifu, na ni lazima mjinyenyekeze na kuleta
kwa Yahweh matoleo kwa moto. 28 Hamtafanya kazi katika siku hiyo kwa sababu ni
Siku ya Upatanisho, ili kufanya upatanisho kwa ajili yenu mbele za Yahweh Mungu
wenu. 29 Yeyote asiyejinyenyekeza siku hiyo lazima akatiliwe mbali na watu wake.
30 Yeye afanyaye kazi yoyote katika siku hiyo, Mimi, Yahweh, nitamwangamiza atoke
miongoni mwa watu wake. 31 Msifanye kazi ya aina yoyote katika siku hiyo. Hii
itakuwa amri ya kudumu katika vizazi vyote vya watu wenu mahali pote mnapoishi.
32 Siku hii itakuwa Sabato ya pumziko lenye utlivu, na ni lzima siku ya tisa ya mwezi
mjinyenyekeze katika majira ya jioni. Tangu jioni hata jioni mtaishika Sabato yenu."
33 Yahweh akazungumza na Musa, akisema, 34 "Zungumza na watu ISraeli, uwaambie
'Katika siku ya kumi na tano ya mwezi wa saba kutakuwa na Sikukuu ya vibanda kwa
Yahweh. nayo itadumu siku saba. 35 Siku ya kwanza kutakuwa na kusanyiko takatifu.
Hamtafanya kazi ya kawaida. 36 Kwa muda wa siku saba mtatoa dhabihu iliyofanywa
kwa moto kwa Yahweh. Siku ya nane kutakuwa na kusanyiko takatifu, nanyi mtato
dhabihu iliyofanywa kwa moto kwa Yahweh. Hili ni kusanyiko lenye utulivu, nanyi
msifanye kazi yoyote ya kawaida. 37 Hizi ndizo sikukuu zilizoamriwa kwa ajili ya
Yahweh, ambazo mnapaswa kuzitangaza kuwa ni makusanyiko matakatifu ya kutoa
dhabihu kwa moto kwa Yahweh, matoleo ya kuteketezwa na matoleo ya nafaka,
dhabihu na matoleo ya vinywaji, kila moja kwa siku yake. 38 Sikukuu hizi zitakuwa
nyongeza kwa Sabato za Yahweh na zawadi zenu, viapo vyenu vyote, na sadaka
zenu zote za hiari mzitoazo kwa Yahweh. 39 Kuhusu Sikukuu ya vibanda, siku ya
kumi na tano ya mwezi wa saba, mtakapokuwa mmeyakusanya ndani matunda ya
nchi, ni lazima muitunze sikukuu hii ya Yehweh kwa muda wa siku saba. Siku ya
kwanza itakuwa ya pumziko lenye utulivu, na siku ya nane pia itakuwa ya pumziko
lenye utulivu. 40 Siku ya kwanza mtachuma tunda lililobora kutoka kwenye miti,
mtakata makuti ya mtende, na matawi ya miti minene yenye majani mengi, na
majani ya mierebi kutoka chemchemi za maji, nanyi mtashangilia mbele za Yahweh

Mungu wenu kwa siku saba. 41 Kwa muda wa siku saba kila mwaka, mtaisherehekea
sikukuu hii kwa Yahweh. Hii itakuwa amri ya kudumu katika vizazi vyote vya watu
wenu mahali popote mtakapoishi. Mtaisherehekea sikukuu hii katika mwezi wa
saba. 42 Mtaishi kwenye vibanda vidogovidogo kwa siku saba. Waisraeli wenyeji
wa kuzaliwa wote itawapasa kuishi katika vibanda vidogovidogo kwa siku saba,
43 ili kwamba wazao wenu, kizazi baada ya kizazi, waweze kujifunza nilivyowafanya
wana wa Israeli kuishi kwenye vibanda kama hivi nilipowaongoza kutoka katika nchi
ya Misri. Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu.'" 44 Katika njia hii Musa akazitangaza
kwa watu wa ISraeli sikukuu zilizoamria kwa ajili ya Yahweh.

# 24

1 Yahweh akamwambia Musa, akisema, 2 "Waamru watu wa Israeli wakuletee
mafuta halisi yaliyokamliwa kutokana na mizeituni ili yatumike kwenye taa, ili
kwamba taa ziweze kuwaka daima na kuleta mwanga. 3 Nje ya pazia lililoko mbele
ya sanduku la maamzi ndani ya hema la kukutania, Aroni ataiwasha daima taa
mbele za Yahweh, tangu asubuhi hata jioni. Hii itakuwa amri ya kudumu katika
vizazi vyote vya watu wenu. 4 Kuhani mkuu atazifanya taa ziwake daima mbele
za Yahweh, taa hizo zilizo kwenye kinara cha dhahabu safi. 5 Yawapasa kuchukua
unga laini na kuoka kwa huo mikate kumi na miwili. Ni lazima kuwe na mbili za
kumi za efa za unga katika kila mkate. 6 Kisha mtaipanga juu ya meza ya dhahabu
safi mbele za Yahweh katika safu mbili, mikate sita katika kila safu, 7 Mtaweka
uvumba safi kando ya kila safu ya mikata kuwa sadaka ya kuwakilisha. Uvumba
huo utachomwa kwa moto kwa ajili ya Yahweh. 8 Kila siku ya Sabato kuhani mkuu
sharti aipange kwa utaratibu hiyo mikate mbele za Yahweh kwa niaba ya watu
wa Israeli, iwe ishara ya agano la milele. 9 Sadaka hii itakuwa kwa ajili ya Aroni
na wanawe, na ni lazima waile mahali palipo patakatifu, kwa kuwa ni sehemu ya
matoleo kwa Yahweh yaliyofanywa kwa moto." 10 Sasa ilitokea kwamba mwana wa
mwanamke Mwisraeli, ambaye baba yake alikuwa Mmisri, alikwenda miongoni mwa
watu wa Israeli. Huyu mwana wa mwanamke Mwisraeli akagombana na mwanume
Mwisraeli kambini. 11 Mwana wa mwanamke Mwisraeli akalikufuru jina la Yahweh
na kumlaani Mungu, kwa hiyo watu wakamleta kwa Musa. Jina la mama yake
aliitwa Shelomithi, binti wa Dibri, kutoka kabila la Dani. 12 Wakamweka kizuizini
mpaka Yahweh mwenyewe atakapotangaza mapenzi yake kwao. 13 Kisha Yahweh
akamwambia Musa, 14 "Mchukue nje ya kambi huyo aliyemlaani Mungu. Wale
wote waliomskia wataweka mikono yao juu ya kichwa chake, na kisha kusanyiko
lote watamponda kwa mawe. 15 Ni lazima uwaeleze watu wa Israeli na kusema,
'Yeyote anayemlaani Mungu wake imempasa kubeba hatia yake mwenyewe. 16 Yeye
anayelikufuru jina la Yahweh kwa hakika ni lazima auawe. Hakika, kusanyiko lote
litampiga mawe, ama awe mgeni au Mwisraeli mwenyeji mzaliwa. Ikiwa yeyote
analikufuru jina la Yahweh, ni lazima auawe. 17 Naye amuuaye mtu mwingine ni
lazima kwa hakika auewa. 18 Yeye anayemuua mnyama wa mwingine sharti amfidie,
uhai kwa uhai. 19 Iwapo mtu anamjeruhi jirani yake, ni lazima atendewe vivyo hivyo
alivyomtendea jirani yake: 20 Mvunjiko kwa mvunjiko, jicho kwa jicho, jino kwa jino.
Kama amesababisha jeraha kwa mtu, ndivyo ipasavyo kutendwa kwake. 21 Yeyote
auaye mnyama ni lazima amfidie, na yeyote auaye mtu ni lazima auawe. 22 Ni lazima
mwe na sheria moja kwa wote, mgeni na Mwisraeli mwenyeji mzaliwa, kwa kuwa
Mimi ndimi Yahweh Mungu wanu." 23 Kwa hiyo Musa akazungumza na watu wa
Israeli, nao watu wakamleta mwanaume huyo nje ya kambi, yule ambaye alikuwa
amemlaani Yahweh. Wakampiga kwa mawe. Watu waisraeli wakaitekeleza amri ya
Yahweh aliyoitoa kupitia Musa.

# 25

[1] Yahweh akazungumza na Musa kwenye Mlima wa Sinai, akisema, [2] "Zungumza
na watu wa Israeli na uwaambie, "Mtakapoingia katika nchi ambayo ninawapa, kisha
hiyo nchi lazima ifanywe iwe ya kuishika Sabato kwa ajili ya Yahweh. [3] Ni lazima
mtapanda mazao yenu kwa miaka sita, na kwa miaka sita mtaikatia matawi mizabibu
yenu na kukusanya mazao yake. [4] Lakini katika mwaka wa saba, Sabato ya pumziko
la utulivu kwa nchi itashikwa, ni Sabato kwa Yahweh. Hamtapanda mashamba
yenu wala kuikatia mizabibu yenu matawi yake. [5] Hamtasimamia mavuno yoyote
ya mazao ya mizabibu iliyojiotesha yenyewe katika mashamba yenu ya mizabibu
isiyokatiwa matawi. Huu utakuwa mwaka wa pumziko lenye utulivu kwa ardhi.
[6] Chochote ardhi isiyofanyiwa kazi itakachotoa wakati wa Sabato ndicho kitakuwa
chakula chako. Wewe mwenyewe, watumwa wako wa kiume na wa kike, watumishi
wako wa kuajiriwa na wageni wanaoishi pamoja nawe mnaweza kujikusanyia
chakula. [7] Na wnyama wako wa kufugwa na wanyama pori waweze kula chochote
ardhi itoacho. [8] Ni lazima kwenu kuhesabu Sabato saba za miaka, yaani, saba
mara miaka saba, ikifanya jumla ya miaka arobaini na tisa. [9] Kisha mtapiga sauti
ya tarumbeta kila mahali katika siku ya kumi ya mwezi wa saba. Katika Siku ya
Upatanisho ni lazima mtapiga tarumbeta katika nchi yenu yote. [10] Nanyi mtautenga
mwaka wa hamsini kwa ajili ya Yahweh na mtatangaza uhuru katika nchi yote kwa
wakazi wote. Kutakuwa na Yubile kwa ajili yenu, ambayo kwayo mali na watumwa ni
lazima warejeshwe kwa familia zao. [11] Mwaka wa saba kutakuwa na Yubile kwenu.
Hamtapanda wala kusimamia mavuno ya kijioteshacho chenyewe, na kukusanya
kichipukacho kwenye mizabibu isiyokatiwa matawi. [12] Kwa sababu hiyo ni Yubile
takatifu kwenu. Nanyi mtakula mazao yanayokua yenyewe kutoka mashambani.
[13] Ni lazima muwarejeshe kila mmoja kwenye miliki yake katika mwaka huu wa
Yubile. [14] Iwapo utauza ardhi yoyote ya jirani yako au kununua ardhi yake, ni shrti
msipunjane au kutendeana kwa hila. [15] Iwapo unanunua ardhi kutoka kwa jirani
yako, zingatia idadi ya miaka na mazao ambayo yaweza kuvunwa mpaka mwaka
wa Yubile nyingine. Jirani yako anayeuza ardhi ni lazima aihesabu miaka hiyo
pia. [16] Miaka inapoongezeka mpaka Yubile nyingine, ataongeza thamani ya ardhi,
na miaka inapokuwa michache kufikia Yubile nyingine atashusha thamani, kwa
sababu idadi ya mavuno inahusiana na idadi ya miaka kabla ya Yubile nyingine.
[17] Msipunjane au kutendeana kwa hila, badala yake, yawapasa kumheshi Yahweh
Mungu wenu. [18] Kwa hiyo basi, ni lazima muyatii maagiza, kuzitunza sheria zangu
na kuzitekeleza. Nanyi mtaishi katika nchi katika usalama. [19] Nayo nchi itawapa
mavuno yake, nanyi mtakula matunda yenu na mtaishi humo salama. [20] Labda
mtasema, Tutakula nini katika mwaka wa saba? Tazama, hatuwezi kupanda wala
kukusanya mazao yetu." [21] Nitaiamru baraaka yangu ije juu yenu katika mwaka
wa sita, nayo itatoa mavuno ya kutosha kwa miaka mitatu. [22] Mtapanda katika
mwaka wa nane na mtaendelea kula mazao ya miaka iliyopita na kutoka kwenye
ghala la chakula. Mpaka mavuno ya mwaka wa tisa yatakapofika, mtaweza kula
kutoka kwenye riziki iliyohifadhiwa katika miaka iliyopita [23] Ardhi haitauzwa kwa
mmiliki mpya wa kudumu, kwa sababu ardhi ni mali yangu. Ninyi nyote mu wageni
na wakazi wa muda juu ya ardhi yangu. [24] Ni lazima muitunze haki ya ukombozi
kwa ajili ya ardhi yote mtakayoimiliki; itawapasa kuruhusu ardhi inunuliwe tena
na familia ambayo wewe uliinunua hiyo ardhi kutoka kwao. [25] Iwapo Mwisraeli
mwenzako anakuwa masikini na kwa sababu hiyo anauza baadhi ya miliki yake,
kisha jamaa yake wa karibu anaweza kuja na kuikomboa hiyo miliki ambayo jamaa
yake kaiuza kwako. [26] Iwapo mtu hana jamaa wa kuikomboa mali yake, lakini ikiwa
kafanikiwa na anao uwezo wa kuikomboa, [27] kisha atahesabu miaka tangu ardhi

hiyo ilipouzwa na kurejesha kwa mtu aliyemuuzia fedha iliyosalia. Naye anaweza
kuerejea kwenye miliki yake mwenyewe. 28 Lakini ikiwa hawezi kuirejesha kwake
ardhi aliyoiuza, nayo hiyo ardhi aliyoiuza itabaki katika umiliki wa yule aliyeinunua
mpaka mwaka wa Yubile. Kwenye mwaka wa Yubile, ardhi itarejeshwa kwa mtu
aliyeiuza, naye mmiliki wa asili atarejea kwenye mali yake. 29 Ikiwa mtu anauza
nyumba iliyo kwenye mji uliozungushiwa ukuta, naye anaweza kuinunua tena ndani
ya mwaka baada ya kuuzwa. kwa kuwa, kwa mwaka mzima atakuwa na haki ya
ukombozi. 30 Kama nyumba hiyo haitakombolewa kabla ya mwaka mzima, ndipo
hiyo nyumba iliyoko kwenye mji uliozungushiwa ukuta itakuwa mali ya kudumu
ya yule aliyeinunua, katika vizazi vyote vya uzao wake. Nyumba hiyo haitakuwa
ya kurejeshwa katika mwaka wa Yubile. 31 Lakini nyumba za vijijini zisizokuwa na
ukuta kuzizunguuka, zitahesabiwa kuwa shamba la nchi. Zaweza kukombolewa, na
ni lazima zirejeshwe katika mwaka wa Yubile. 32 Hata hivyo, nyumba zinazomilikiwa
na makuhani katika miji yao zaweza kukombelewa wakati wowote. 33 Iwapo mmoja
wa makuhani haikombowi nyumba iliyozwa, kisha nyumba hiyo iliyouzwa katika
miji ilimo, ni lazima irejeshwe katika mwaka wa Yubile, kwa kuwa nyumba za miji
ya makuhani ni mali yao miongoni mwa watu wa Israeli. 34 Lakini yale mashamba
yanayozunguka miji yao hayataweza kuuzwa kwa sababu hiyo ni mali ya kudumu
ya Makuhani. 35 Ikiwa mwananchi mwenzako anakuwa masikini, kiasi kwamba
hawezi kujihudumia, nawe utalazimika kumsaidia kama vile ungemsaidia mgeni au
mwingine yeyote kutoka nje aishie miongoni mwenu. 36 Usimtoze riba au kujaribu
kunufaika kutoka kwake katika njia yoyote, bali mheshimu Mungu wako ili kwamba
ndugu yako aendelee kuishi nawe. 37 Hutampa mkopo wa fedha na kumtoza riba,
wala hutamuuzia chakula chako ili kupata faida. 38 Mimi ndimi Yahweh Mungu
wako, aliye kuleta wewe kutoka nchi ya Misri, ili kwamba Nikupe nchi ya Kanaani,
na kwamba niwe Mungu wako. 39 Iwapo mwananchi mwenzako atakuwa masikini
na kujiuza mwenyewe kwako, hutamfanyisha kazi kama mtumwa. 40 Mtendee
kama mtumishi wa kuajiriwa. Ni lazima awe kama yule ahudumuye nawe kwa
muda mpaka mwaka wa Yubile. 41 Kisha ataondoka kwako, yeye mwenyewe na
watoto wake pamoja naye, na atarejea kwenye familia yake mwenyewe na kwenye
miliki ya baba yake. 42 Kwa sababu wao ni watumishi wangu niliowaleta kutoka
katika nchi ya Misri. Hawatauzwa kama watumwa. 43 Usitawale juu yao kwa
ukatili, bali yakupasa kumheshimu Mungu wako. 44 Kwa upande wa watumwa
wako wakiume na watumwa wako wa kike, unaowezao kuwapata kutok kwa mataifa
yanayokuzunguka, waweza kununua watumwa kutoka kwao. 45 Unaweza pia
kununua watumwa kutoka kwa wageni wanaoishi miongoni mwenu, yaani, kutoka
familia zao waliopamoja nawe, wale wtoto waliozaliwa katika nchi yako. Wanaweza
kuwa mali yako. 46 Unaweza kuzalisha watumwa hao kama urithi kwa watoto wako
baada yako, ili kuwamiliki kama mali. Kutoka kwao waweza kununua watumwa
daima, lakini hamtawezi kutawala kwa ukali juu ya ndugu zenu walio miogoni mwa
watu wa Israeli. 47 Iwapo mgeni anayeishi nawe kwa muda anakuwa tajiri, na
ikiwa mmoja wa Waisraeli amekuwa masikini na kujuza mwenyewe kwa familia
ya mgeni, au kwa mtu fulani katika familia, 48 baada ya Mwisraeli mwenzako kuwa
amenunuliwa. Anaweza kurejeshwa kwa maliopo. Iwapo anaweza kurejeshwa. Mtu
fulani katika familia yake anaweza kumkomboa. 49 Anaweza kuwa mjomba wake, au
mjomba wa mwanawe, anayemkomboa yeye, au yeyote aliye ndugu yake wa karibu
kutoka kwa ukoo wake. Au, iwapo ni mwenye mafanikio, anaweza kujikomboa
mwenyewe. 50 Ni lazima apatane na mtu aliyemnunua, itawapasa kuhesabu miaka
tangu mwaka aliojiuza kwa mnunuzi wake mpaka mwaka wa Yubile. Ile thamani ya
ukombozi wake ihesabiwe kulingana na kiwango cha mshahara anaolipwa mtumishi

aliyeajiriwa, kwa idadi ya miaka ambayo angeweza kuendelea kufanya kazi kwa yule
aliyemnunua. 51 Endapo kutakuwa kungali na miaka mingi iliyobaki mpaka mwaka
wa Yubile, atalazimika kulipa fungu kubwa la fedha kwa ajili ya ukombozi ambao ni
uwino wa idadi ya miaka hiyo. 52 Iwapo kuna miaka michache tu iliyobaki mpaka
mwaka wa Yubile, atapatana na aliyemnunua ili kuipitia idadi ya miaka iliyobaki
mpaka Yubile, naye atalazimika kulipia ukombozi wake kulingana na idadi ya
miaka. 53 Naye atatendewa kama mtu aliyeajiriwa mwaka kwa mwaka. Utahakikisha
kwamba hatendewi kwa ukali. 54 Iwapo hakukombolewa katika njia hizi, basi
atatumika mpaka mwaka wa Yubile, yeye pamoja na watoto wake. 55 Kwangu mimi
watu wa Israeli ni watumishi. Wao ni watumishi wangu ambao Niliwatoa katika nchi
ya Misri. Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu.

# 26

1 Msijitengenezee sanamu, wala msisimamishe kinyago cha kuchonga au nguzo
ya jiwe ya kuabudia, na msisimamisha sura ya jiwe la kuchonga katika nchi
yenu mtayoiinamia, kwa kuwa Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu. 2 Ni lazima
muitunze Sabato Yangu na kupaheshimu patakatifu pangu. Mimi ndimi Yahweh.
3 Iwapo mtatembea katika sheria zangu na kuzishika amri zangu na kuzitii, 4 Nami
nitawapa ninyi mvua katika majira yake; nayo nchi itatoa mazao yake, na miti
ya shambani itatoa matunda yake. 5 Upuraji wenu utaendelea hata wakati wa
mavuno ya zabibu, na mavuno ya zabibu yataendelea mpaka majira ya kupada
mbegu. Nanyi mtakula mkate na kushiba na kuishi salama mahali mtakapofanya
mji wenu katika nchi. 6 Nitawapa amani; mtalala bila ya kitu chochote kuwatia
hofu. Nitawaondolea mbali wanyama waliohatari katika nchi, na upanga hautapita
katika nchi yenu. 7 Mtawafukuza adui zenu, nao wataanguka mbele yenu kwa
upanga. 8 Watu wenu watano watafukuza adui mia moja, na watu wenu mia
moja watafukuza adui elfu kumi; adui zenu wataanguka mbele yenu kwa upanga.
9 Nitawatazama kwa upendeleo na kuwafanya nyinyi mzae na kuwazidisha nyinyi.
10 Mtakula chakula kilichotunzwa ghalani kwa muda mrefu. Mtayaondoa mazao
yaliyohifadhiwa ghalani kwa sababu mtahitaji ghala kwa ajili ya mavuno mapya.
11 Nitaliweka hema langu katikati yenu, nami stachukizwa nanyi. 12 Nitatembea
miongoni mwenu nami nitakuwa Mungu wenu, nanyi mtakuwa watu wangu.
13 Mimi ndimi Yahweh Mungu wenu, aliyewaleta nyinyi kutoka nchi ya Misri, ili
kwamba msingeendelea kuwa watumwa wao. Nimevunja makomeo ya nira yenu na
nikawafanya mtembee kwa kunyooka. 14 Lakini ikiwa hamtanisikiliza mimi, 15 na
kutozitii amri hizi, na ikiwa mtayakataa maagizo yangu, na kuzichukia sana sheria
zangu, kiasi kwamba hamtaweza kuzitii amri zangu zote, lakini mkalivunja agano
langu— 16 —kama mtafanya mambo haya, Nami nitafanya hili kwenu: Nitasababisha
hofu juu yenu, maradhi na homa kali itakayoangamiza macho na kuondoa uhai
wenu. Mtapanda mbegu zenu kwa hasara, kwa sababu adui zenu watakula mazao
yake. 17 Nitakaza uso wangu dhidi yenu, na mtashindwa na adui zenu. Watu
wanaowachukia watatawala juu yenu, na mtakimbia hata kama hakutakuwa na
yeyote anayewafukuza. 18 Iwapo hamtasikiliza maagizo yangu, Nami niwataadhibu
vikali mara saba kwa dhambi zenu. 19 Nami nitakivunja kiburi chenu katika
uwezo wenu. Nitaifanya mbingu juu yenu iwe kama chuma na nchi yenu kama
shaba. 20 Nguvu yenu itatumika bure, kwa sababu nchi yenu haitazalisha mavuno
yake, na miti yenu katika nchi haitazaa matunda yake. 21 Iwapo mtataenenda
kinyume changu na hamtanisikiliza mimi, nitaleta mapigo mara saba zaidi juu
yenu, sawasawa na dhambi zenu. 22 Nitatuma wanyama mapori hatari dhidi yenu,
ambao watawaibia watoto wenu, kuangamiza mifugo yenu na kuwafanya mwe

wachache katika idadi yenu. Hivyo barabara zenu zitakuwa nyeupe. 23 Endapo
pamoja na mambo haya kuwapata lakini msiyakubali marekebisho yangu na mkazidi
kuenenda katika upinzani dhidi yangu, 24 ndipo nami pia nitaenenda kinyume
chenu, na Mimi mwenyewe nitawaadhibu mara saba kwa sababu ya dhambi
zenu. 25 Nitaleta upanga juu yenu utakaowaadhibu kwa kisasi kwa sababu ya
kulivunja agano. Nanyi mtajikusanya kwenye miji yenu, Nami nitatuma humo maafa
miongoni mwenu, na mtachukuliwa mikononi mwa adui yenu. 26 Nitakapokomesha
mgao wa chakula, wanawake kumi wataweza kuoka mkate wako katika chombo
kimoja cha kuokea na watakugawia mkate wako kwa uzani. Nanyi mtakula lakini
hamtatoshelezwa. 27 Endapo hamtanisikiliza pamoja na mambo haya kuwapata,
lakini mkazidi kuenenda kinyume na mimi, 28 kisha nami nitakwenda kinyume
nanyi katika hasira, Nami nitawaadhibu hata mara saba kulingana na wingi wa
dhambi zenu. 29 Ndipo mtakapokula nyama ya wana wenu; mtakula nyama ya
binti zenu. 30 Nitapaangamiza mahali penu pa juu, kuziangusha chini madhabahu
zenu za kufukizia uvumba, na kuzitupa maiti zenu juu ya maiti ya sanamu zenu, na
Mimi mwenyewe nitawadharau nyinyi. 31 Nitaigeuza miji yennu kuwa magofu na
kupaharibu patakatifu penu. Nami sitapendezwa na harufu nzuri ya matoleo yenu.
32 Nami nitaiharibu nchi. Adui zenu watakaokuwa wakiishi humo watashtushwa na
uharibifu huo. 33 Nami nitawatawanya nyinyi katika mataifa, na nitaufuta upanga
wangu na kuwafuatia. Nchi yenu itatelekezwa, na miji yenu itakuwa magofu. 34 Nayo
nchi itazifurahia Sabato zake kwa kuwa itakuwa imetelekezwa na ninyi mkiwa
katika nchi za daui zenu. Katika nyakati hizo, nchi itapumzika na kufurahia Sabato
zake. 35 Maadamu itakuwa imetelekezwa, itakuwa na pumziko, ambalo litakuwa ni
pumziko iliyolikosa pamoja na Sabato zenu mlipokuwa mkiishi ndani yake. 36 Na kwa
wale watakoachwa humo kwenye nchi za adui zenu, Nitatuma hofu ndani ya mioyo
yenu kiasi kwamba hata kama ni maelfu ya majani tu yatakapopeperushwa katika
upepo yatawaogofyeni. Nanyi mtaanguka hata kama hakutakuwa na awafukuzaye.
37 Mtajikwaa kila mmoja juu ya mwenzake kama vile mlikuwa mkiukimbia upanga,
hata kama hakutakuwa na awafukuzaye nyinyi. Hamtakuwa na nguvu ya kusimama
mbele ya daui zenu. 38 Nanyi mtaangamia miongoni mwa mataifa, nayo nchi ya
adui zenu yenyewe itawamezani. 39 Wale watakosalia miongoni mwenu watapotelea
katika dhambi zao, huko kwenye nchi za adui zenu, na kwa sababu ya dhambi
zao, na kwa sababu ya dhambi za baba zao watapotelea mbali pia. 40 Lakini
kama watakiri dhambi zao na dhambi ya baba zao, na usaliti wao ambao kwao
hawakuwa waaminifu kwangu, pia na mwenendo wao dhidi yangu— 41 ambao
ulinisababisha kuwa kinyume nao, na kuwaleta katika nchi ya adui zao—iwapo
mioyo yao isiyotahiriwa itanynyekezwa, 42 na iwapo wataikubali adhabu kwa ajili
ya dhambi zao, nami nitalikumbuka agano langu na Yakobo, agano langu na Isaka,
agano langu na Abrahamu; Pia, nitaikumbuka nchi. 43 Nchi itakayotelekezwa na wao,
hivyo itapendezwa na Sabato zake inapobaki imetelekezwa na wao. Itawapasa kulipa
hatia kwa dhambi zao kwa sababu ni wao wenyewe ndiyo walioyakataa maagizo
yangu na kuzichukia sheria zangu. 44 Lakini pamoja na haya yote, watapokuwa katika
nchi ya adui zao, Mimi stawakataa wao, wala sitawachukia ili kuwaangamiza kabisa
na kulifutilia mbali agano langu nilililoagana nao, kwa kuwa Mimi ndimi Yahweh
Mungu wao. 45 Bali kwa ajili yao, nitalikumbuka agano langu na baba zao, niliowaleta
kutoka katika nchi ya Misri machoni pa mataifa, ili niwe Mungu wao. Mimi ndimi
Yahweh." 46 Hizi ndizo amri, hukumu, na sheria ambazo Yahweh alifanya baina yake
na watu wa Israeli kwenye Mlima Sinai kwa kupitia Musa.

# 27

1 Yahweh akazungumza na Musa na akasema, 2 “Zungumza na watu wa Israeli
na uwaambie, 'Iwapo mtu yeyote anatoa kiapo maalum cha kuwa mnathiri kwa
Yahweh, tumieni tathmini zifuatazo: 3 Viwango vyenu vya thamani kwa mwanaume
aliye na umri kati ya miaka ishirini na miaka sitini yaweza kuwa shekeli hamsini za
fedha, kulingana na vipimo vya shekeli ya mahali pa patakatifu. 4 Kwa mwanamke
wa umri uleule viwango vyenu vya thamani yapasa viwe shekeli thelathini vya
fedha. 5 Tangu wenye umri wa miaka mitano mpaka wa miaka ishirini viwango
vyenu vya thamani kwa mwananume vitakuwa shekeli ishirini za fedha, na kwa
mwanamke ni shekeli kumi za fedha, 6 Kwa wenye umri wa tangu mwezi mmoja
mpaka miaka mitano viwango vyenu vya thamani kwa mawanaume vitakuwa shekeli
tano za fedha na kwa mwanamke shekeli tatu za fedha. 7 Tangu wenye umri
wa miaka sitini na zaidi kwa mwanaume viwango vyenu vya thamani vitakuwa
shekeli kumi na tano, na kwa mwanamke ni shekeli kumi. 8 Lakini kama mtu
atoaye kiapo cha mnadhiri hawezi kulipa kiwango hicho cha thamani, kisha huyo
mtu anayetolewa lazima atapelekwa kwa kuhani, naye kuhani atamthamanisha
huyo atolewaye kwa kiasi anachoweza kutoa yule anayetoa kiapo cha mnadhiri.
9 Iwapo mtu anataka kutoa sadaka ya mnyama kwa Yahweh, na iwapo Yahweh
ataikubali, kisha huyo mnyama atatengwa kwake. 10 Mtu huyo hataruhusiwa kumtoa
madhabahuni au kumbadilisha huyo mnyama, mzuri kwa mbaya au mbaya kwa
mzuri. endapo atatoa mnyama badala ya mwingine, kisha wanyama hao wawili;
yule anayetolewa na yule anayebadilishwa wanakuwa watakatifu. 11 Hata hivyo,
iwapo kile mtu amishaapa kumtolea Yahweh kwa uhalisia siyo kisafi, kwa hiyo,
Yahweh hatakikubali, naye huyo mtu atalazimika kumleta huyo mnyama kwa kuhani.
12 Kuhani atamthamanisha, kwa thamani ya soko la mnyama. Thamani yoyote kuhani
atakayoiweka juu ya mnyama, hiyo ndiyo itakuwa thamani yake. 13 Na kama mmiliki
anapenda kumkomboa, kisha tano ya thamani yake itaongezwa kwenye gharama
yake ya ukombozi. 14 Mtu aitengapo nyumba yake iwe zawadi takatifu kwa Yahweh,
kisha kuhani ataweka thamani yake ama iwe ni nzuri au mbaya. Thamani yoyote
itakayowekwa na kuhani juu yake, ndiyo itakuwa thamani yake. 15 Lakini kama
mmiliki wake anayeitenga nyumba yake anapenda kuikomboa, atalazimika kuongeza
sehemu ya tano ya thamani yake kwenye gharama ya ukombozi wake, nayo nyumba
itakuwa yake. 16 Iwapo mtu anatenga sehemu ya ardhi yake mwenye, kisha tathmini
yake itakuwa katika uwiano kwa kiwango cha kiasi cha mbegu inayotakiwa kuipanda
katika ardhi hiyo—homeri moja ya mbegu za shairi ambayo itathamanishwa kwa
shekeli hamsini za fedha. 17 Na kama analitenga shamba lake katika mwaka wa
Yubile, tathmini yake ya awali itabaki kuwa ileile. 18 Lakini endapo atalitenga shamba
hilo baada ya mwaka wa Yubile, kisha kuhani atalazimika kukokotoa thamani yake
kwa idadi ya miaka inayobaki mpaka mwaka wa Yubile, na thamani yake lazima
ishushwe. 19 Iwapo mtu anayelitenga shamba lake anapenda kuliko, mboa, naye
atalazimika kuongeza sehemu ya tano kwenye thamani, nalo shamba litakuwa
lake tena. 20 Iwapo halikomboi shamba, au iwapo amishaliuza shamba kwa mtu
mwingine, haliwezi kukombolewa tena. 21 Badala yake, shamba hilo litakapoachwa
huru katika mwaka wa Yubile, litakuwa zawadi takatifu kwa Yahweh, kama lilivyo
shamba lililotolewa kabisa kwa Yahweh. Nalo litakuwa mali ya kuhani. 22 Iwapo
mtu anatenga shamba alilolinunua, lakini hilo shamba siyo sehemu ya ardhi ya
familia yake, 23 kuhani atafanya tathmini yake mpaka mwaka wa Yubile, na mtu
huyo lazima atalipa thamani yake katika siku hiyo hiyo kuwa zawadi takatifu kwa
Yahweh. 24 Katika mwaka wa Yubile, shamba litarejeshwa kwa mtu yule ambaye
lilikuwa limenunuliwa, kwa mmiliki wa ardhi. 25 Tathmani yote lazima ifanywe

kwa uzani wa shekeli ya mahali pa patakatifu. Gera ishirini kwa shekeli moja.
26 Asiwepo mtu atakayetenga mzaliwa wa kwanza miongoni mwa wanyama, kwa
kuwa wazaliwa wote wa kwanza wa wanyama tayari ni mali ya Yahweh; iwe ni
maksai au kondoo, ni wa Yahweh. 27 Na kama ni mnyama aliye najisi, kisha mmiliki
wake anaweza kumnunua tena sawasawa na thamani yake, na sehemu ya tano
lazima itaongezwa kwenye thamani hiyo. Na kama mnyama hakombolewi, naye
atauzwa kwa thamani iliyowekwa. 28 Hakutakuwa na kitu amabacho mtu anakitoa
kwa Yahweh, kutoka katika vyote alivyonavyo, iwe ni mwanadamu au mnyama,
au ardhi ya familia yake, ambacho chaweza kuuzwa au kukombolewa. Kila kitu
kitolewacho ni kitakatifu sana kwa Yahweh. 29 Hakuna fidia inayoweza kulipwa kwa
ajili ya mtu aliyetolewa ili kuangamizwa. Mtu huyo sharti auawe 30 Zaka yote iliyo
ya ardhini, iwe nafaka ichipukayo juu ya ardhi au tunda kutoka kwenye miti, ni mali
ya Yahweh. Ni takatifu kwa Yahweh. 31 Iwapo mtu anakomboa chochote cha zaka
yake, atalazimika kuongeza sehemu ya tano kwenye thamani yake. 32 Na kwa kila
mnyama wa kumi wa kundi la ng'ombe au la kondoo, yeyote anayepita chini ya fimbo
ya mchungaji, atatengwa kwa ajili ya Yahweh. 33 Mchungaji hatatafuta wanyma
waliobora au wabaya kabisa, na haruhusiwi kubadili mnyama mmoja kwa mnyama
mwingine. Iwapo anambadilisha kwa namna yoyote ile, kisha wote wawili yule
wa kwanza na huyo aliyebadiliwa watakuwa watakatifu. Mnyama huyo atolewaye
hawezi kukombolewa.'" 34 Hizi ndizo amri ambazo Yahweh alimpa Musa kwenye
mlima Sinai kwa ajili ya watu wa Israeli.

# Hesabu

1 Mungu alimwambia Musa katika hema ya kukutania walipokuwa katika jangwa
la Sinai. Hii ilitokea katika siku ya kwanza ya mwezi wa pili miaka miwili baadaya
Waisraeli kutoka nchi ya Misri. Mungu alisema, 2 'fanya sensa ya wanaume wote
wa Israel kutoka kila ukoo, katika familia za baba zao. Wahesabu kwa majina,
wahesabu kila mume, kila mwanamume 3 kuanzia umri a miaka ishirini na zaidi.
Uwahesabu wote wanaoweza kupigana kama askari wa Israel. Wewe na Haruni
mtaandika idadi ya wanaume katika makundi ya majeshi yao. 4 Kila mwanamume
kwa kila kabila, kichwa cha ukoo, lazima atumike na wewe kama kiongozi wa kabila.
5 Haya ndiyo majina ya viongozi ambao watapigana pamoja na wewe: Kutoka kabila
la Reubeni, Elizuri mwana wa Shedeuri; 6 kutoka kabila la Simeoni, Shelumiel mwana
wa Zurishadai 7 Kutoka kabila la Yuda, Nashoni mwana wa Aminadabu; 8 Ktoka
kabila la Isakari, Nethaneli mwana wa Zuari; 9 kutoka kabila Zebuluni, Eliabu mwana
wa Heloni 10 kutoka kabila la Efraimu mwana wa Yusufu, Elishama mwana wa
Ammihudi; kutoka kabila la Manase, Gamaliel mwan wa Pedazuri; 11 kutoka kabila
la Benjamini mwana wa Ysufu, Abidani mwan wa Gidion; 12 Kutoka kabila la Dan,
Ahizeri mwana wa Amishadai; 13 kutoka kabila Asheri, Pagieli mwana wa Okirani;
14 kutoka kabila la Gadi, Eliasafu mwana wa Deuli; 15 na kutoka kabila la Naftali,
Ahira mwana wa Enani." 16 Hawa ndio wanaume waliochaguliwa kutoka kwa watu.
Waliongoza kabila za mababu zao. Walikuwa viongozi wa koo katika Israel. 17 Musa
na Haruni wakawachukua wale wanaume, waliokuwa wameandikwa kwa majina,
18 na pamoja na wanaume hao waliwakusanya wanume wote katika siku ya kwanza
ya mwezi wa pili. Kisha kila mwanume wa miaka ishirini na zaidi alitambua babu
zake. Alitakiwa kutaja koo na famila kutoka katika ukoo. 19 Kisha Musa akaandika
hesabu yao huko katika nyika ya Sinai, Kama Mungu alivyokuwa amemwamuru
kufanya. 20 Kutoka uzao wa Reubeni, mtoto wa kwanza wa Israel, yalihesabiwa
majina yote ya kila mwanamume mwenye umri wa miaka ishirini na zaidi wenye
uwezo wa kwenda vitani, kutoka hesabu ya ukoo na familia. 21 Waliwahesabu
wanaume 46, 000 kutoka ukoo wa Reubeni. 22 Kutoka uzao wa Simeoni yalihesabiwa
majina yote ya kila mwanamume mwenye umri wa miaka ishirini na zaidi au wenye
uwezo wa kwenda vitani, kutokana na hesabu ya ukoo na familia. 23 Walihesabu
wanaume 59, 300 kutoka kabila la Simeoni. 24 Kutoka uzao wa Gadi yalihesabiwa
majina yote ya kila mwanamume mwenye umri wa miaka ishirini au zaidi na wenye
uwezo wa kwenda vitani, kutoka kwenye hesabu ya ukoo na familia. 25 Walihesabu
wanaume 45, 650 kutoka kabila la Gadi. 26 Kutoka uzao wa Yuda yalihesabiwa majina
yote ya wanaume wenye umri wa miaka ishirini au zaidi na wenye uwezo wa kwenda
vitani, kutoka kwenye hesabu ya ukoo na familia. 27 walihesabiwa wanume 74, 000
kutoka kabila la Yuda. 28 Kutoka uzao wa Isakari yalihesabiwa majina yote ya kila
mwanamume mwenye umri wa miaka ishirini au zaidi na wenye uwezo wa kwenda
vitani, kutoka kwenye hesabu ya ukoo na familia. 29 Walihesabiwa wanaume 54,
000 kutoka kabila la Isakari. 30 Kutoka uzao wa Zabuloni yalihesabiwa majina yote
ya kila mwanamume mwenye umri wa miaka ishirini au zaidi na wenye uwezo
wa kwenda vitani, kutoka kwenye hesabu ya ukoo na familia. 31 Walihesabiwa
wanume 57, 400 kutoka kabila la Zabuloni. 32 Kutoka uzao wa Efraimu mwana
wa Yusufu yalihesabiwa majina yote ya kila mwanaume mwenye umri wa miaka
ishirini au zaidi na wenye uwezo wa kwenda vitani, kutoka kwenye hesabu ya ukoo
na familia. 33 Walihesabiwa wanaume 40, 500 kutoka kabila la Efraimu. 34 Kutoka
uzao wa Manase mwana wa Yusufu yaliheabiwa majina yote ya kila mwanaume

mwenye umri wa miaka ishirini au zaidi na wenye uwezo wa kwenda vitani, kutoka
kwenye hesabu y a ukoo na familia. 35 Walihesabiwa wanaume 32, 000 kutoka
kabila la Manase. 36 Kutoka uzao wa Benjamini yalihesabiwa majina yote ya kila
mwanaume mwenye umri wa miaka ishirini au zaidi na wenye uwezo wa kwenda
vitani, kutoka kwenye hesabu ya ukoo na familia. 37 Walihesabiwa wanaume 35, 000
kutoka kabila la Benjamini. 38 Kutoka uzao wa Dani yalihesabiwa majina yote ya kila
mwanaume mwenye umri wa miaka ishirini au zaidi na mwenye uwezo wa kwenda
vitani, Kutoka kwenye hesabu ya ukoo na familia. 39 Walihesabiwa wanaume 62, 000
kutoka kabila la Dani. 40 Kutoka uzao wa Asheri yalihesabiwa majina yote ya kila
mwanume mwenye umri wa miaka ishirini au zadi na mwenye uwezo wa kwenda
vitani, kutoka kwenye hesabu y a ukoo na familia. 41 Walihesabiwa wanaume 41,
500 kutoka ukoo wa Asheri. 42 Kutoka ukoo wa Naftali yalihesabiwa majina yote
ya kila mwanaume mwenye umri wa miaka ishirini au zaidi na mwenye uwezo
wa kwenda vitani, kutoka kwenye hesabu ya ukoo na familia. 43 Walihesabiwa
wanaume 53, 400 kutoka kabila la Naftari 44 Musa na Haruni waliwahesabu wanaume
wote hawa, pamoja na wale wanaume kumi na wawili waliokuwa wakiongoza yale
makabila kumi na mawili ya Israeli. 45 Kwa hiyo wanaume wote wa Israeli wenye
umri wa miak ishirini au zaidi, wote wenye uwezo wa kwenda vitani, walihesabiwa
kutoka kwenye familia zao. 46 Walihesabu wanaume 603, 550. 47 Lakini wanaume
toka uzao wa Lawi hawakuhesabiwa, 48 Kwa sababu BWANA alimwambia Musa,
49 “usiwahesabu wale wa kabila la Lawi wala kuwajumuisha kwenye jumla ya
watu wa Israeli. 50 Badala yake, waagize Walawi kuliangalia hema la amri za
agano, na kuangalia mapambo ya hema na vyote vilivyomo. Walawi watalazimika
kulibeba hema na lazima wayabebe mapambo ya hema. Lazima waliangalie hema
na kuyatengeneza mazingira yake. Wataiangalia masikani na kuzitengeneza kambi
zinazolizunguka. 51 Kila hema litakapotakiwa kuhamishiwa eneo jingine, Walawi
ndio watakaolipeleka pale. Na kila hema litakapotakiwa kusimamishwa, Walawi
ndio watakao lisimamisha. Na mgeni yeyote atakayelisogelea hema lazima auawe.
52 Wakati watu wa Israeli watakaposimamisha hema zao, kila mwanaume lazima
awe karibu na bango la jeshi lake. 53 Hata hivyo Walawi lazima waweke hema zao
kuizunguka hiyo masikani ya amri za agano ili kwamba hasira yangu isije ikawaka
juu ya wana wa Israeli. Walawi lazima wailinde hiyo masikani ya amri za agano.”
54 Wana wa Israeli walifanya yote haya. Walifanya yote ambayo BWANA aliagiza
kupitia Musa.

# 2

1 BWANA akasema na Musa na Haruni tena. Akamwambia, 2 Kila mtu atapanga
kulingana na mahali pake, pamoja na mabango ya baba zao. Watapanga kuzunguka
hema ya kukutania kila upande. 3 Wale watakaopanga mashariki mwa hema ya
kukutania, mahali ambapo juu huonekana wakati wa jua kuchomoza, ni makambi
ya Yuda nao watakuwa katika kundi lao. Nashoni mwana wa Aminadabu ni kiongozi
wa watu wa Yuda. 4 Idadi ya watu wa Yuda ni 74, 600. 5 Kabila la Isakari litapanga
mbele ya Yuda. Nethaneli mwana wa Zuari ataliongoza jeshi la Isakari. 6 Idadi ya
kikosi chake ni wanaume 54, 000. 7 Kabila la Zabuloni litapanga mbele ya Isakari.
Eliabu mwana wa Heloni ndiye atakayeliongoza jeshi la Zabuloni. 8 Idadi ya kikosi
chake ni 57, 400. 9 Idadi yote ya kambi y a Yuda ni 186, 400. Watakuwa wa kwanza
kuondoka. 10 Upande wa kusini kutakuwa na kambi ya Reubeni katika kundi lao.
Kiongozi wa kundi la Reubeni ni Elizuri mwana wa Shedeuri. 11 Idadi ya kikosi
chake ni 46, 500. 12 Simeoni atapanga mbele ya Reubeni. Kiongozi wa watu wa
Simeoni ni Shelumieli mwana wa Zurishadai. 13 Waliohesabiwa kwenye kikosi chake

ni 59, 300. [14] Kabila la Gadi litafuatia. Kiongozi wa watu wa Gadi ni Eliasafu mwana
wa Deuli. [15] Idadi ya kikosi chake ni 45, 650. [16] Wote waliohesabiwa kwenye kambi
ya Reubeni, kulingana na kikosi chake, ni 151, 450. Watakuwa wa pili kuondoka.
[17] Kifuatacho, ni hema la kukutania kuondoka kambini pamoja na Walawi likiwa
katikati ya kambi zote. Lazima waondoke hapo kambini kwa mpangilio huo kama
walivyoingia kwenye kambi. Kila mwanamume lazima awe mahali pake kwa kufuata
bango lake. [18] Migawanyiko ya kambi y Efraimu kufuata mahali pake. Kiongozi wa
watu wa Efraimu ni Elishama mwana wa Amihudi. [19] Hesabu ya kikosi hiki ni 40,
500. [20] Baada ya hao lilifuata kabila la Manase. Kiongozi wa Manase ni Gamaliel
mwana wa Pedazuri. [21] Hesabu ya kikosi hiki ni 32, 200. [22] Kabila litakalofuata ni
la Benjamini. Kiongozi wa Benjamini n Abidani mwana wa Gidioni. [23] Hesabu ya
kikosi hiki ni 35, 000 [24] Wote waliohesabiwa katika kambi ya Efraimu ni 108, 100.
Watakuwa wa tatu kuondoka. [25] Upande wa kaskazini kutakuwa na kambi ya kikosi
cha Dani. Kiongozi wa watu wa Dani ni Ahiezeri mwana wa Amishadai. [26] Hesabu
ya kikosi hiki ni 62, 700. [27] Watu wa kabila ya Asheri watapanga mbele ya Dani.
Kiongozi wa Asheri ni Pagieli mwana wa Okirani. [28] Hesabu ya Kikosi hiki ni 41,
500. [29] Kabila la Naftali ndilo litakalofuatia. Kiongozi wa Naftali ni Ahira mwana
wa Enani. [30] Hesabu ya kikosi hiki ni 53, 400. [31] Wote waliohesabiwa kwenye kambi
ya Dani ni 157, 600. Hawa watakuwa wa mwisho kuondoka kambini, wakifuata
bango lao. [32] Hawa ndio Waisraeli, waliohesabiwa kufuata familia zao. Wote
waliohesabiwa kwenye kambi zao, kwa kufuata vikosi vyao ni 603, 550. [33] Lakini
Musa na Haruni hawakujumuisha Walawi kwenye Hesabu ya Waisrael. Ilikuwa kama
BWANA alivyokuwa amemwagiza Musa. [34] Watu wa Israel walifanya yote ambayo
BWANA alimwagiza Musa. Walipanga kwa kufuata mabango yao. Walisafiri kutoka
kambini kwa kufuata jamaa zao, kwa mpangilio wa familia za koo zao.

# 3

[1] Sasa hii ndiyo historia ya uzao wa Haruni na Musa wakati BWANA aliposema
na Musa kwenye mlima Sinai. [2] Majina ya watoto wa Haruni walikuwa Nadabu
ambaye ndiyo mtoto wa kwanza, na Abihu, na Eliezeri, na Ithamari. [3] Haya
ndiyo majina ya wana wa Haruni, makuhani waliokuwa wamepakwa mafuta na
kuwekwa wakfu kutumika kama makuhani. [4] Lakini Nadabu na Abihu walikufa
mbele ya BWANA walipomtolea moto usiokubalika walipokuwa katika nyika ya Sinai.
Nadabu na Abihu hawakuwa na watoto, kwa hiyo Eliazari na Ithamari walitumika
kama makuhani pamoja na baba yao. [5] BWANA alinena na Musa, akamwambia,
[6] “Walete kabila ya Lawi na uwaweke kwa Haruni kuhani ili wamsaidie [7] Nao lazima
wafanye majukumu badala ya Haruni na jumuiya yote mbele ya hema ya kukutania.
Lazima watumike hemani. [8] Watayatunza mapambo ya hema ya kukutania, na
watawatumikia makabila ya Israel kwa huduma ya hemani. [9] Uwaweke Walawi
kwa Haruni na watoto wake. Nimewatoa kikamilifu ili wamsaidie kuwatumikia
watu wa Israel. [10] Umchague Haruni na watoto wake kuwa makuhani, lakini mgeni
yeyote atakayekaribia lazima auawe.” [11] BWANA alinena na Musa. akamwambia,
[12] “Tazama, nimewachagua Walawi katika watu wa Israel. Nimefanya hivyo badala
ya kuchukua mzaliwa wa kwanza wa kiume wa wana wa Israel. Hawa Walawi
ni wangu. [13] Na hata wazaliwa wa kwanza ni mali yangu. Katika siku ambyo
niliwavamia wazaliwa wote wa kwanza wa nchi ya Misri, Niliwatenga wazaliwa
wa kwanza wa Israeli kwa ajili yangu, watu na wanyama pia. Ni mali yangu.
Mimi ndimi BWANA.” [14] BWANA alinena na Musa katika nyika ya Sinai. Akasema,
[15] “Wahesabu uzao wa Lawi katika kila familia, katika nyumba za koo zao. Hesabu
kila mume kuanzia mwezi mmoja au zaidi.” [16] Musa aliwahesabu, kufuata maelekezo

ya BWANA, kama alivyoamriwa kufanya. [17] Majina ya watoto waLawi yalikuwa
Gerishoni, Kohathi, na Merari. [18] Ukoo uliotokana na watoto wa Gerishoni walikuwa
ni Libni na Shimei. [19] Ukoo uliotokana na watoto Kohathi walikuwa ni Amramu na,
Izihari, Hebroni, na Uzieli. [20] Ukoo uliotokana na watoto wa Merari walikuwa ni
Mahili na Mushi. Hizi ndizo koo za Walawi, zilizoorodheshwa ukoo kwa ukoo. [21] Koo
za Walibini na Washimei zilitokana na Wagerishoni. Hizi ndizo koo za Wagerishoni.
[22] Wanaume wote wenye umri wa mwezi mmoja au zaidi walihesabiwa na kufikia
idadi ya 7, 500. [23] Koo za Wagerishoni watapanga upande wa magharibi wa hema.
[24] Eliasafu mwana wa Laeli ataongoza koo za uzao wa Wagerishoni. [25] Familia ya
Gerishoni watalilinda hema la kukutania pamoja na hiyo masikani. Watalilinda
hema, kifuniko chake, na lile pazia la lango la hema ya kukutania. [26] Wataulinda
ua, lile pazia la kwenye lango—ua unaozunguka mahali patakatifu na madhabahu.
Watazilinda kamba za hema ya kukutania na vyote vilivyomo. [27] Koo zifuatazo
zinatokana na Kohathi: ukoo wa Waamrami, ukoo wa Waizihari ukoo wa Wahebroni,
na ukoo wa Wauzieli. Koo hizi zinatokana na Wakohathi. [28] Wanaume 8, 600 wenye
umri wa mwezi mmoja au zaidi walihesabiwa ili kulinda vitu vya BWANA. [29] Familia
ya uzao wa Kohathi watapanga upande wa kusini wa Hema. [30] Elizafani mwana
wa Uzieli ndiye atakayeongoza ukoo wa Wakohathi. [31] Watalilinda sanduku, meza,
vikalishio vya taa, madhabahu, vitu vitakatifu ambvyo hutumika katika huduma
yao, pazia, na kazi zote zinazoambatana na hema. [32] Eliazari mwana wa Haruni
kuhani atawaongoza wanaume wanaowaongoza Walawi. Atawasimamia wanaume
wanaongoza eneo takatifu. [33] Koo mbili zimetoka kwa Merari: Ukoo wa Mahili na
ukoo wa Mushi. Koo hizi zimetokana na Merari, [34] Wanaume 6, 200 wenye umri
wa mwezi mmoja na zaidi walihesabiwa. [35] Zurieli mwana wa Abihaili ataongoza
ukoo wa Merari. Hawa watapanga upande wa kaskazini mwa hema. [36] Uzao wa
Merari utatunza mbao za hema, mataruma, nguzo, makalishio, viifaa vya ujenzi
na vitu vyote vinavyohusika, [37] na nguzo za ua zinazozunguka hema, makalishio,
vigingi na kamba zake. [38] Musa na Haruni na watoto wake watapanga upande wa
mashariki wa masikani, mbele ya hema ya kukutania kuelekea mawio ya jua. Wao
wataajibika na majukumu ya mahali patakatifu na majukumu ya wana wa Israeli.
Mgeni atakayekaribia mahali patakatifu auawe. [39] Musa na Haruni wakawahesabu
wanaume wote wa ukoo wa Walawi walikuwa na umri wa mwezi mmoja na zaidi,
kama vile BWANA alivyokuwa ameagiza.. Walihesabu wanaume ishirini na mbili
elfu. [40] BWANA alisema na Musa, “Wahesabu wanaume wote ambo ni wazaliwa wa
kwanza wa Israeli ambao wana umri wa mwezi mmoja na zaidi. Orodhesha majina
yao. [41] Unitwalie walawi kwa ajili yangu badala ya wazaliwa wa kwanza wa Israeli,
Mimi ndimi BWANA. Na utwae wanyama wa Walawi badala ya wazaliwa wa kwanza
wa wanyama wa uzao wa Israeli,” [42] Musa akawahesabu wazaliwa wa kwanza wote
wa Israeli kama BWANA alivyomwagiza kufanya. [43] Aliwahesabu wazaliwa wote wa
kwanza kwa mjina, wenye umri wa mwezi mmoja na zaidi. Alihesabu wanaume
22, 273. [44] Tena BWANA alinena na Musa. Akasema, [45] “Watwae Walawi badala ya
wazaliwa wote wa kwanza wa wana wa Israeli. Na utwae wanyama wa Walawi
badala ya wanyama wa Waisreli wengine. Walawi ni mali yangu. Mimi ndimi
BWANA. [46] Unikusanyie shekeli tano za wokovu kwa kila hao 273 za hao wazaliwa wa
kwanza wa Israeli za hao wanaozidi idadi ya Walawi. [47] Utazitumia hizo shekeli tano
kwa kipimo cha mahali patakatifu. Shekeli moja ni sawa na gera ishirini. [48] Utawalipa
hizo shekeli za wokovu kwa Haruni na wanawe.” [49] Kwa hiyo Musa akakusanya
shakeli za wokovu kutoka kwa wale waliozidi idadi ya wale waliookolewa na Walawi.
[50] Musa akakusanya zile fedha kutoka kwa hao wazaliwa wa kwanza wa wana wa
Israeli. Alikusanya jumla ya shekeli 1, 365, zenye kipimo sawa na mahali patakatifu.

Musa akamlipa Haruni na wanawe hizo shekeli za wokovu. 51 Musa akafanya kila
kitu alichoagizwa na neno la BWANA kama BWANA alivyomwagiza.

# 4

1 BWANA akanena na Musa na Haruni. Akasema, 2 Fanya sensa ya uzao waume wa
Kohathi kutoka kwa Walawi, kwa kufuata jamaa na na familia za koo. 3 Uwahesabu
wanaume ambao wana umri wa miaka thelathini hadi miaka hamsini. Hawa
wataungana na kundi linalotumika kutoa huduma kwenye hema ya kukutania.
4 Uzao wa Kohathi watalinda vile vitu vitakatifu zaidi vilivyohifadhiwa kwa ajili
yangu katika hema ya kukutania. 5 Wakati kambi inapojiandaa kusonga mbele,
Haruni na wanawe lazima waende hemani, kulishusha pazia linalotenganisha mahali
patakatifu na kulifunika sanduku la ushuhuda kwa pazia hilo. Watalifunika hilo
sanduku kwa ngozi za pomboo. 6 Watatandika juu yake nguo za rangi ya samawi.
Watachomeka hiyo miti ya kubebea. 7 Watatandika nguo ya rangi ya samawi kwenye
meza ya mikate ya wonyesho. Juu yake wataweka sahani, vijiko, mabakuli na
vikombe vya kumiminia. Mikate itakuwepo daima mezani. 8 Wataifunika na nguo ya
rangi nyekundu na ngozi za pomboo. na kuweka miti ya kubebea. 9 Watachukua
nguo ya rangi ya samawi na kukifunika kinara, pamoja na taa zake, na koleo
zake, na sahani zake na vikombe vyake vya kuwekea mafuta ya taa. 10 Wataweka
kinara na vifaa vyake vikiwa vimefunikwa na ngozi ya pomboo, na wataweka
kwenye miti ya kukibebea. 11 Watafunika na nguo ya samawi katika madhabau
ya dhahabu. Wataifunika na ngozi za pomboo, na kuweka ile miti ya kubebea.
12 Watavichukua vyombo vyote vya kazi takatifu na kuvizonga kwenye hiyo nguo
ya rangi ya samawi. Watavifunika na ngozi za pomboo na kuviweka hivyo vyombo
kwenye miti ya kubebea. 13 Watayaondoa majivu kwenye madhabahu na kutandika
nguo ya rangi ya zambarau juu yake. 14 Watavieka kwenye miti ya kubebea
vyombo vyote wanavyovitumia kwa kazi ya madhabahuni. Vyombo hivi ni vyetezo,
majembe, mabakuli na vitu vingine vya madhabahuni. Wataifuniks madhabahu na
ngozi za pomboo na kuweka ile miti ya kubebea. 15 Wakati Haruni na wanawe
walipokuwa wamekamilisha kupafunika mahali patakatifu na vyombo vyote, na
kambi itakapoanza kuendelea mbele, ndipo wana wa Kohathi watakapokuja kubeba
vitu vya mahali patakatifu. Kama watagusa vyombo vitakatifu, lazima watakufa.
Hii ni kazi ya wana wa uzao wa Kohathi, kubeba mapambo ya hema ya kukutania.
16 Eliazari mwana wa Haruni kuhani atalinda na kusimamia mafuta ya taa, ubani
mzuri, sadaka za mara kwa mara na mafuta ya upako. Atasimamia ulinzi wa hema
lote na vyote vilivyomo, mahali patakatifu na vyombo vyake." 17 BWANA akanena
na Musa na Haruni. Akasema, 18 Usiruhusu kabila la Wakohathi kuondolewa kati
ya Walawi. 19 Walinde waishi ili wasije wakafa, kwa kufanya hivi. Wanapokuwa
wanasogelea 20 wasije wakaingia ndani ili kuona eneo takatifu hata kwa kitambo,
vinginevyo watakufa. Bali Haruni na wanawe wanaweza kuingia, ndipo Haruni na
Wanawe watakapowapangia Wakohathi kazi maalumu ya kufanya, kwa kila mmoj."
21 BWANA akanena na Musa tena, Akasema, "Fanya sensa kwa wana Gerishoni pia,
kwa kufuata familia za mababu zao, koo zao. 22 Uwahesabu wale wenye umri
wa mika thelathini hadi miaka hamsini. 23 Uwahesabu wote ili waje kuungana na
wale wanaotumika katika hema ya kukutania. 24 Hii ndiyo itakuwa kazi ya koo za
Gerishoni, wanapotumikia na wanachobeba. 25 Watabeba pazia la masikani, hema
la kukutania, na vifunikio vyake, vifuniko vya ngozi ya pomboo ambvyo viko juu
yake, na pazia kwenye lango la hema ya kukutania. 26 Watabeba pazia la ua, pazia la
kwenye mlango wa ua, ambao uko karibu na maskani karibu na madhabahu, kamba
zake na vifaa vyote vya utumishi wake. Chochote kinachotakiwa kufanywa kutokana

na vitu hivi, wao ndio watakaofanya. [27] Haruni na wanawe ndio watakaoongoza
utumishi wa uzao wa Wagerishoni, kwa vitu vyote vile vya kusafirisha, na katika
utumishi wao wote. Lazima uwagawie majukumu yao yote. [28] Huu ndio utumishi
wa koo za uzao wa wana wa Wagerishoni katka hema ya kukutania. Ithamari
mwana wa Haruni kuhani atawaongoza katika utumishi. [29] Utawahesabu uzao wa
Merari kwa koo zao, na uwapange katika familia za mabau zao, [30] kuanzia wenye
umri wa miaka thelatini hadi miaka hamsini. Umuhesabu kila atakayeungana na
kundi lenye utumishi katika hema ya kukutania. [31] Huu ndio wajibu na kazi yao
katika utumishi wao kwenye hema ya kukutania. Watazilinda mbao za maskani,
mataluma yake, nguzo na makalishio yake, [32] pamoja na nguzo za ua zinazozunguka
masikani, makalishio yake, vigingi na kamba zake, na vifaa vinginevya ujenzi.
Waorodheshe kwa majina na majukumu yao. [33] Huu ndio utumishi wa koo za uzao
wa Merari, ambao wanatakiwa kufanya katika hema ya kukutania, chini ya uongozi
wa Ithmari mwana wa Haruni kuhani." [34] Musa na Haruni na viongozi wa watu
waliwahesabu wana wa uzao wa Wakohathi kwa kufuata koo za familia za mababu
zao. [35] Waliwahesabu wale wenye umri wa miaka thelathini hadi miaka hamsini.
Walimhesabu kila mmoja aliyepaswa kuungana na kundi linalotoa huduma ya
utumishi kwenye hema ya kukutania. [36] Waliwahesabu wanaume 2, 750 kwa kufuata
koo zao. [37] Musa na Haruni waliwahesabu wanaume wote kutoka koo na familia
za Wakohathi ambao hutumika kwenye hema ya kukutania. Walifanya hivi kwa
kumtii BWANA aliyewaagiza kupitia kwa Musa. [38] Uzao wa Gerishoni walihesabiwa
kufuata koo na familia za mababu zao, [39] kuanzia umri wa miaka thelathini hadi
miaka hamsini, kwa kila mmoja aliyetakiwa kuungana na watu wanaotoa huduma
kwenye hema ya kukutania. [40] Wanaume wote waliohesabiwa kufuata koo na
familia za mababu zao walikuwa 2, 630. [41] Musa na Haruni walizihesabu koo
za uzao wa Gerishoni ambao watatumika kwenye hema ya kukutania. Walifanya
hivi ili kutii ambacho BWANA aliwaamuru kufanya kuptia kwa Musa. [42] Uzao wa
Merari walihesabiwa kwa koo kupitia familia za mababu zao, [43] kuanzia wenye
umri wa miaka thelathini hadi miaka hamsini, kila anayepaswa kuungana na
watu wanaotumika kwenye hema ya kukutania. [44] Wanaume wote waliohesabiwa
kupitia koo za familia za mababu zao walikuwa 3. 200. [45] Musa na Haruni
waliwahesabu wanaume hawa, uzao wa Merari. Kw kufanya hivi walitii amri ya
BWANA aliyowaaagiza kufanya kupitia kwa Musa. [46] Kwa hiyo Musa na Haruni na
viongozi wa Israeli waliwahesabu Walawi wote kw kufuata koo na familia za mababu
zao [47] kuanzia wenye umri wa miaka thelathini hadi miaka hamsini. walimhesabu
kila aliyepaswa kufanya kazi kwenye masikani, na kila aliyepaswa kubeba na kulinda
vitu vya kwenye hema ya kukutania. [48] Waliwahesabu wanaume 8, 580. [49] Kwa
agizo la BWANA, Musa alimhesabu kila mwanamume na kutunza kumbukumbu ya
kazi ambayo kila mmoja anaweza kufanya. Kwa hivyo, walitii kile ambacho BWANA
alikuwa amewaagiza kufanya kupitia kwa Musa.

# 5

[1] BWANA alinena na Musa. Akasema, [2] "Waamuru wana wa Israel wawatoe
watu wote wenye magonjwa ya ngozi yanayoambukiza, na kila mwenye mwenye
vidonda vinavyotoa harufu, na ambaye amenajisika kwa kugusa maiti. [3] Awe mme
au mke, umtoa kambini. Ili wasije wakaitia unajisi kambi, kwa sababu Mimi huishi
ndani yake," [4] Watu wa Israeli walifanya hivyo. Waliwatoa kambini, Kama BWANA
alivyomwagiza Musa. Watu wa Israeli walimtii BWANA. [5] Tena BWANA akanena na
Musa. Akasema, [6] "Nena na wana wa Israeli. mtu mume na mtu mke akifanya
dhambi yeyote ambayo watu hufanyiana wao kwa wao, na mtu huyo akamwasi

BWANA, mtu huyo atakuwa na hatia. 7 Ndipo huyo mtu ataungama hiyo dhambi
aliyoifanya. Mtu huyo atarudisha malipo ya hatia yake na kuongeza kwenye malipo
hayo sehemu ya tano zaidi. Atamlipa huyo aliyemtendea makosa 8 Lakini kama
huyo mtu huyu aliyetendewa kosa hana ndugu wa kupokea hayo malipo, basi
atalipa hayo malipo ya hatia kwangu kupitia kuhani pamoja na kondoo dume kwa
ajili ya sadaka yake mwenyewe. 9 Kila sadaka ya wana wa Israeli, vitu ambavyo
vimetengwa na vikaletwa kwa kuhani na watu wa Israeli, vitakuwa vyake. 10 Sadaka
ya kila mtu itakuwa ya kuhani; kama mtu yeyote atatoa kitu chochote kwa kuhani,
kitakuwa chake." 11 Tena BWANA akanena na Musa. Akasema, 12 "Nena na wana
wa Israel. Uwaambie, 'kama mke wa mtu ataasi na kufanya dhambi dhidi ya
mume wake. 13 Halafu mtu mwingine akalala naye. Kwa sababu, hiyo atakuwa
amenajisika. Na hata kama mume wake hakuona na hajui, hata kama hakuna mtu
aliyemkamta akiwa katika tendo na hakuna mtu wa kushuhudia dhidi yake; hata
hivyo ile roho ya wivu itaendele kumjulisha yule mume kuwa mke wake amenajisika.
14 Ingawa, roho ya wivu inaweza kumdanganya yule mwanamume wakati mke wake
hajanajisika. 15 Kwa mazingira hayo, yule mwanamume anapaswa kumpeleka mke
wake kwa kuhani. Yule mwanamume anapaswa kutoa sadaka ya divai kwa ajili
yake. Atapaswa kuleta sehemu ya kumi ya efa ya unga wa shayiri. Asitie mafuta
juu yake wala asitie ubani juu yake maana ni sadaka ya unga ya wivu, ni sadaka
ya unga ya ukumbusho wa uovu. 16 Ndipo kuhani atasogeza karibu na kumweka
mbele ya BWANA. 17 Kuhani atachukua kikombe cha maji matakatifu na atachukua
mavumbi ya kwenye masikani. Ataweka yale mavumbi kwenye maji. 18 Kisha kuhani
atamweka huyo mwanamke mbele za BWANA na atazifungua nywele kichwani kwa
huyo mwanamke. Atamwekea mikononi mwake hiyo sadaka ya unga kwa ajili ya
ukumbusho, ambayo ni sadaka ya unga kwa ajili ya wivu. 19 Kuhani atashikilia
mikononi mwake maji machungu yanayoweza kuleta laana. Kuhani atamweka huyo
mwanamke chini ya kiapo na kumwambia. 'Kama haujafanya uzinzi na mwanaume
mwingine, na kama hajakengeuka na kufanya uovu, basi utakuwa huru na maji
haya yanayoweza kuleta laana. 20 Lakini kama wewe, mwanamke uliye chini ya
mume wako, umekengeuka, na kama umenajisika, na kama mwanamume mwingina
amelala nawe, 21 ndipo, (kuhani atamtaka huyo mwanamke aape kiapo kinachoweza
kuleta laana kwake, na kwamba ataendelea kumwambia yule mwanamke) 'BWANA
atakufanya wewe kuwa laana itakayooneshwa kuwa hivyo kwa watu wako. Hii
itatokea pale BWANA atakapoyafanya mapaja yako kuoza na tumbo lako kuvimba.
22 Haya maji ambayo huleta laana yataingia tumboni mwako na kulifanya tumbo
lako kuvimba na mapaja yako kuoza,' mwanamke alitakiwa kujibu, 'Ndiyo, hayo
yanipate kama mimi ni mwenye hatia.' 23 Naye kuhani ataziandika laana hizi kwenye
kitabu, na kisha kuzifuta laana zilizoandikwa kwa maji ya uchungu. 24 Naye kuhani
atamwelekeza yule mwanamke kunywa yale maji machungu yaletayo laana. Yale
maji yaletayo laana yataingia na kuwa machungu. 25 Kuhani ataitwaa ile sadaka ya
unga ya wivu mikononi mwa yule mwanamke. Atailekeza ile sadaka ya unga mbele
ya BWANA na kuileta madhabahuni. 26 Kuhani atachukua konzi ya sadaka ya unga
mkononi mwake kama sadaka ya kuwakilisha, na kuiteketeza madhabahuni. Ndipo
atakapompatia mwanamke yale maji machungu ili ayanywe. 27 Wakati wa kumpa
yale maji ili anywe, kama amenajisika kwa sababu alifanya uovu dhidi ya mume
wake, ndipo yale maji yaletayo laana yatamwingia na kuwa machungu. Tumbo
lake litavimba na paja lake litaoza. Yule mwanamke atalaaniwa kati ya watu wake.
28 Lakini kama yule mwanake hajanajisika na kama ni msafi, basi atakuwa huru.
Tena ataweza kubeba uja uzito. 29 Hii ndiyo sheria ya wivu. Ni sheria ya mwanamke
anayekengeuka kwa mumewe na kunajisika. 30 Ni sheria ya mwanamume mwenye

roho ya wivu kwa mkewe. Atamleta mwanamke mbele ya BWANA, na kuhani
atamfanyia huyo mwanamke kila kitu ambacho sheria ya wivu inamtaka kufanya.
31 Yule mwanamume atakuwa hana hatia kwa kumleta mke wake kwa kuhani. Na
yule mwanmke atauchukua uovu wake.”

# 6

1 BWANA alinena na Musa. Akamwabia, 2 'Nena na wana wa Israeli, uwaambie,
'Kama mume au mke ataweka nadhiri kwa BWANA kwa kiapo maalumu cha
mnadhiri, ndipo atajiepusha na divai na vileo. hatakunywa siki itokanayo na divai.
3 Asinywe kileo kitokanacho na siki au kilevi. Asinywe maji ya divai yeyote au kula
zabibu mbichi wala zilizokauka. 4 Katika siku zote ambazo amejitenga kwa ajili
yangu, asile chochote kinachotokana na zabibu, wala kitu chochote kitokanacho na
makokwa hadi maganda. 5 Wakati wote wa nadhiri yake, wembe usiipite kichwani
mwake mpaka siku zake za nadhiri kwa BWANA zitimilike. Lazima ajitenge kwa
BWANA. Ataziacha nywele zake zikue kichwani mwake. 6 Wakati wote wa kujidhiri
kwake kwa BWANA, asiikaribie maiti. 7 Asijinajisi kwa namna yeyote hata kama
atakufa baba yake, mama, dada, au ndugu yake. Hii ni kwa sababu amejitenga
kwa ajili ya Mungu, kama ambavyo kila mmoja anavyoweza kumuona kwa uerfu
wa nywele zake. 8 Wakati wote wa kujidhiri kwake atakuwa mtakatifu, alijitunza
kwa ajili ya BWANA. 9 Ikitokea mtu amekufa ghafla pembeni yake na kukitia unajisi
kichwa chake kitakatifu, ndipo atakaponyoa kichwa chake katika siku ya kujitakasa
—Siku ya saba atanyoa kichwa chake. 10 Siku ya nane atamletea kuhani njiwa
wawili au makinda mawili ya njiwa kwenye lango la hema ya kukutania. 11 Naye
kuhani atamtoa ndege mmoja kama sadaka ya dhambi na mwingine kama sadaka ya
kuteketezwa. Hawa watafanyika sadaka ya upatanisho kwake kwa sababu atakuwa
ametenda dhambi ya kuwa karibu na mfu. Atatakasika kichwa chake siku hiyo.
12 Atajitenga kwa BWANA tena katika siku hizo za utakaso. Ataleta kondoo mume
mwenye umri wa mwaka mmoja kama sadaka ya hatia. Zile siku zake kabla ya
kunajisika hazitahesabiwa, kwa sababu kujiweka wakfu kwake kulinajisika. 13 Hii
ndiyo sheria ya mnadhiri wakati wa muda wa kujidhiri unapokuwa umetimia.
Ataletwa kwenye mlango wa hema ya kukutania. 14 Ataleta sadaka yake kwa
BWANA. Atatoa mwanakondoo mume wa mwaka mmoja asiye na hila kama sadaka
ya kuteketezwa. Ataleta kondoo mke wa mwaka mmoja asiye na hila kama sadaka ya
dhambi. Ataleta kondoo mume asiye na hila kama sadaka ya amani. 15 Ataleta kikapu
cha mikate iliyotengenezwa bila amira, mikate ya unga mwembamba iliyokandwa
kwa mafuta, mikate ya kaki isiyo na amira iliyopakwa mafuta, pamoja na sadaka
za unga na sadaka za vinywaji. 16 Kuhani atawaleta mbele za BWANA. Atazitoa
hizo sadaka zake za dhambi na kuteketezwa. 17 Na kikapu cha mikate isiyowekwa
amira, atamtoa yule kondoo mume kama sadaka ya amani kwa BWANA. Pia kuhani
atatoa hiyo sadaka ya unga na sadaka ya vinywaji. 18 Mnadhiri atanyoa nywele
zake kama ishara ya kujitenga kwa ajili ya Mungu kwenye mlango wa hema ya
kukutania. Atazitoa nywele zake kichwani kwake na kuzichoma kwa moto ulio
chini ya sadaka ya amani. 19 Kuhani atachukua bega la kondoo mume lililotokoswa,
na mkate usiotiwa amira toka kikapuni, na mkate mmoja wa kaki usiotiwa amira.
Atauweka kwenye mikono ya Mnadhiri baada ya kuwa amenyoa nywele kwa ishara
ya kujidhiri. 20 Kisha kuhani atavitikisa kuwa sadaka kwa BWANA, sehemu takatifu
kwa kuhani, pamoja na kidari cha kutikiswa na paja lililotolewa kwa kwa kuhani.
Baadaye, Mnadhiri anaweza kunywa divai. 21 Hii ndiyo sheri ya Mnadhiri anayeapia
sadaka yake kwa BWANA kwa ajili ya kujidhiri kwake. Chochote atakachotoa, lazima
afanye kama alivyoapa, kuilinda ahadi yake kama ilivyoaniswa katika sheria ya

Mnadhiri. 22 Tena BWANA akanena na Musa, akasema, 23 “nena na Harunu na
wanawe. Uwaambie, 'mtawabariki wana wa Israeli kwa njia hii. Mtawaambia,
24 BWANA na awabariki na kuwatunza. 25 BWANA na awaangazie nuru ya uso wake
na awe mwenye neema kwenu. 26 BWANA na awatazame kwa neema na awape
amani.'” 27 Ni kwa jinsi hii kwamba wanaweza kuwapa jina langu wana wa Israeli.”

# 7

1 Siku ambayo Musa alikamilsha masikani, alitia mafuta na kuiweka wakfu kwa
BWANA, pamoja na mapambo yake. Aliifanyia hivyo madhabahu na vyombo vyake.
Aliitia mafuta na kuiweka wakfu kwa BWANA. 2 Siku hiyo, viongozi wa Israeli na wale
vichwa vya familia za mababu walitoa sadaka. Hawa wanaume walikuwa viongozi
wa makabila. Walisaidia kuhesabu watu kwenye ile sensa. 3 Walileta sadaka zao kwa
BWANA. Walileta magari sita yaliyofunikwa na mafahari kumi na mbili. Walileta gari
moja kwa kila viongozi wawili, kila kiongozi alileta fahari moja. Walileta vitu hivi
mbele ya masikani. 4 Kisha BWANA akanena na Musa, akamwambia, 5 “Uzipokee
hizo sadaka kutoka kwao na uzitumie kwa matumizi ya kazi ya hema ya kukutania.
Uwape hizo sadaka Walawi, kwa kila mmoja kadri ya uhitaji wa kazi yake.” 6 Musa
akayatwaa yale magari na mafahari. na kuwapatia Walawi. 7 Aliwapa magari
mawili na mafahari wanne wale wa uzao wa Gerishoni, kwa sababu ndivyo kazi yao
ilivyohitaji. 8 Aliwapatia uzao wa Merari magari manne na mafahari nane, chini ya
uangalizi wa Ithamari mwana wa Haruni kuhani. Alifanya hivi kwa sababu ya uhitaji
wa kazi yao. 9 Lakini wale wa uzao wa Kohathi hakuwapa chochote kwa sababu
wao waliangalia vitu vtakatifu amabvyo vilipaswa vibebwe mabagani mwao, siyo
kwa magari. 10 Viongozi walitoa bidhaa zo zingine kwa ajili ya kuwekwa wakfu kwa
madhabahu katika siku ile ambayo Musa aliitia mafuta madhabahu. Viongozi walitoa
sadaka zao mbele ya madhabahu hiyo. 11 BWANA akasema na Musa, “kila kiongozi
atatoa sadaka kwa siku yake kwa ajili ya kuiweka wakfu madhabahu.” 12 Katika
siku ya kwanza, Nashoni mwana wa Aminadabu, wa kabila ya Yuda, alitoa sadaka
yake. 13 Sadaka yake ilikuwa sahani moja ya fedha yenye uzani wa shekeli 130 na
bakuli moja ya fedha ambayo uzito wake ni shekeli sabini, kwa kipimo cha mahali
patakatifu. Vyombo vyote hivi vilikuwa vimejaa unga mwembamba uliochanganywa
na mafuta kuwa sadaka ya unga. 14 Pia alimpa unga wa dhahabu kiasi cha bakuli
moja chenye uzani wa shekeli kumi kilichojaa ubani 15 Alitoa sadaka ya kuteketezwa
fahari mchanga, kondoo dume mmoja na mwanakondoo dume mmoja wa mwaka
mmoja. 16 Alitoa beberu kama kama sadaka ya hatia. 17 Alitoa makisai mbili, kondoo
waume watano, beberu watano na wanakondoo dume watano wenye umri wa
mwaka mmoja mmoja, kama sadaka ya amani. Hii ilikuwa sadaka ya Nashoni mwana
wa Aminadabu. 18 Siku ya pili, Nethanel mwana wa Zuari, kiongozi wa Isakari, alitoa
sadaka yake. 19 Sadaka yake ilikuwa sahani moja ya fedha ya uzito wa shekeli130 na
bakuli moja la fedha lenye uzani wa sheli sabini, kwa kipimo cha mahali patakatifu.
Viyombo vyote hivi vilikuwa vimejaa unga mwembamba uliochanganywa na mafuta
kwa sadaka ya unga. 20 Pia alitoa kijiko kimoja cha dhahabu chenye uzito wa
shekeli kumi, iliyojaa ubani. 21 Alitoa sadaka ya kuteketezwa fahari mchanga, kondoo
dume mmoja, na mwanakondoo mmoja dume. 22 Alitoa beberu mmoja kuwa sadaka
ya dhambi. 23 Alitoa makisai wawili, Kondoo dume watano, beberu watano, na
wanakondoo dume watano wa mwaka mmoja mmoja kuwa sadaka ya amani. Hiii
likuwa sadaka ya Nethaneli mwana wa Zuari. 24 Siku ya tatu, Eliabu mwana wa
Heloni, kiongozi wa uzao wa Zabuloni alitoa sadaka yake. 25 Sadaka yake ilikuwa
sahani moja ya fedha yenye uzani wa shekeli 130, na bakuli moja la fedha lenye
uzito wa shekeli sabini kwa kipimo cha shekeli za mahali patakatifu. vyombo vyote

hivi vilikuwa vimeja unga mwembemba uliochanganywa na mafuta kuwa sadaka
ya unga. 26 Pia alitoa kijiko kimoja cha dhahabu chenye uzani wa shekeli kumi,
kilichojaa ubani. 27 Alitoa sadaka ya fahari mchanga, kondoo dume mmoja, na
mwanakondoo dume mmoja. 28 Alitoa beberu mmoja kama sadaka ya dhambi.
29 Alitoa makisai wawili, kondoo dume watano, beberu watano, na wanakondoo
dume watano wa mwaka mmoja mmoja. kuwa sadaka ya amani. Hii ilikuwa sadaka
ya Eliabu mwana Heloni. 30 Siku ya nne, Elizuri mwana wa shedeuri, kiongozi
wa uzao wa Reubeni, alitoa sadaka yake. 31 Sadaka yake ilikuwa sahani moja ya
fedha yenye uzani wa shekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzani wa shekeli
sabini, kwa kipimo cha shekeli za mahali patakatifu. Vyombo hivi vyote vilikuwa
vimejaa unga mwembamba uliochanganywa na mafuta kuwa sadaka ya unga. 32 Pia
alitoa kijiko kimoja cha dhahabu chenye uzani wa shekeli kumi, kilichoo jaa ubani.
33 Alitoa sadaka ya kuteketezwa fahari mmoja mchanga, mwanakondoo dume mmoja
mchanga wa mwaka mmoja. 34 Alitoa beberu moja kuwa sadaka ya dhambi. 35 Alitoa
maksai wawili, kondoo dume watano wa mwaka mmoja kuwa sadaka ya amani. Hii
ilikuwa sadaka ya Elizuri mwana wa Shedeuri. 36 Siku ya tano, Shelumieli mwana wa
Zurishadai, kiongozi wa uzao wa Simeoni, alitoa sadaka yake. 37 Sadaka yake ilikuwa
sahani moja ya fedha yenye uzani wa shaekali 130 na bakuli mojala fedha lenye uzani
wa shekeli sabini kwa kipimo cha shekeli za mahali patakatifu. Vyombo vyote hivi
vilikuwa vimejaa unga mwembamba uliochanganywa na mafuta kuwa sadaka ya
unga. 38 Pia alitoa kijiko kimoja cha dhahabu chenye uzani wa shekeli kumi, uliojaa
ubani. 39 Alitoa sadaka ya kuteketezwa fahari mchanga, dume la kondoo, na dume
la mwanakondoo la mwaka mmoja. 40 Alitoa beberu moja kuwa sadaka ya dhambi.
41 Alitao maksai wawili, dume wawili wa kondoo, beberu watano, na dume watano
wa wanakondoo wa mwaka mmoja mmoja kuwa sadaka y amani. Hiindiyo iliyokuwa
sadka ya Shelumei mwana wa Zurishadai. 42 Siku ya sita, Eliasafu mwana wa Deuli,
kiongozi wa uzao wa Gadi, alitoa sadaka yake. 43 Sadaka yake ilikuwa sahani moja ya
fedha yenye uzani wa shekeli 130 na bakuli la shaba lenye uzani wa shekeli sabini,
kwa kipimo cha shekeli za mahali patakatifu. Vyombo hivi vyote vilikuwa vimejaa
unga mwembemba uliochanganywa na mafuta kwa ajili ya sadaka ya unga. 44 Pia
alitoa kijiko kimoja cha dhahabu chenye uzani wa shekeli kumi, kilichojaa ubani.
45 Alitoa sadaka ya kuteketezwa ya fahari changa, kondoo dume mmoja, na dume
la mwanakondoo mmoja wa mwaka mmoja. 46 Alitoa beberu mmoja kuwa sadaka
ya dhambi. 47 Alitoa maksai wawili, dume watano wa kondoo, beberu watano, na
wanakondoo dume watano wa mwaka mmoja kuwa sadaka ya amani. Hii ndiyo
iliyokuwa sadaka ya Eliasafu mwana wa Deuli. 48 Siku ya saba, Elishama mwana
wa Amihudi, kiongozi wa uzao wa Efraimu, alitoa sadaka yake. 49 Sadaka yake
ilikuwa sahani moja ya fedha yenye uzani wa shekeli 130 na bakuli la fedha lenye
uzani wa shekeli sabini, kwa kipimo cha shekeli za mahali patakatifu. Vyombo hivi
vyote ilikuwa vimejaa unga mwembamba uliochanganywa na mafuta kuwa sadaka
ya unga. 50 Pia alitoa kijiko kimoja cha dhahabu, kilichojaa ubani 51 Alitoa sadaka ya
kuteketezwa, fahari mmoja, kondoo dume mmoja, na mwanakondoo dume mmoja
wa mwaka mmoja. 52 Alitoa beberu mmoja kuwa sadaka ya dhambi. 53 Alitoa maksai
wawili, kondo dume watano, beberu watano, na na wanakondoo dume watano wa
mwaka mmoja mmoja kuwa sadaka ya amani. Hii ndiyo ilikuwa sdaka ya Elishama
mwana wa Amidu. 54 Siku y a nane, Gamaliel mwana wa Pedazuri, kiongozi wa
uzao wa Manase, alitoa sadaka yake. 55 Sadaka yake ilikuwa sahani moja ya fedha
yenye uzani wa shekeli130 na bakuli moja la fedha lenye uzani wa shekeli sabini,
kwa kipimo cha shekeli za mahali patakatifu. Vyombo vyote hivi vilikuwa vimejaa
unga mwembamba uliochanganywa na mafuta kuwa sadaka ya unga. 56 Pia alitoa

kijiko kimoja cha dhahabu chenye uzani wa shekeli kumi, kilichojaa ubani. 57 Alitoa
sadaka ya kuteketezwa ya fahari mmoja, kondoo dume mmoja, na mwanakondoo
dume mmoja wa mwaka mmoja. 58 Alitoa beberu mmoja kuwa sadaka ya dhambi.
59 Alitoa maksai wawili, kondoo dume watano, beberu watano, na wanakondoo dume
watano wa mwaka mmoja mmoja kuwa sadaka ya amani. Hii ndiyo iliyokuwa sadaka
ya Gamaliel mwana wa Pedazuri. 60 Siku ya tisa, Abidani mwana wa Gidioni, kiongozi
wa uzao wa Benjamini, alitoa sadaka yake. 61 Sadaka yake ilikuwa sahani moja
yafedha yenye uzani wa sheli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzito wa shekeli
sabini, kwa kipimo cha shekeli za mahali patakatifu. Vyombo vyote hivi vilikuwa
vimejaa unga mwembamba uliochanganywa na mafuta kuwa sadaka ya unga. 62 Pia
alitoa kijiko kimoja cha dhahabu chenye uzani wa shekeli kumi, kilichojaa ubani.
63 Alitoa sadaka ya kuteketezwa fahari mmoja mchanga, kondoo dume mmoja, na
mwanakondoo dume mmoja wa mwaka mmoja. 64 Alitoa beberu mmoja kuwa sadaka
ya dhambi. 65 Alitoa makisai wawili, kondoo dume watano, beberu watano, na
wanakondoo dume watano kuwa sadaka ya amani. Hii ndiyo iliyokuwa sadaka ya
Abidani mwana wa Gidioni. 66 Siku ya kumi, Ahizeri mwana wa Amishadai kiongozi
wa Dani alitoa sadaka yake. 67 Alitoa sahani moja ya fedha yenye uzani wa shaekeli
130 na bakuli moja lenye uzani wa shekeli sabini, kwa kipimo cha shekeli za mahali
patakatifu. Vyombo vyote hivi vilikuwa vimejaa unga mwembamba uliochanganywa
na mafuta kuwa sadaka ya unga. 68 Pia alitoa kijiko kimoja cha dhahabu chenye
uzito wa shekeli kumi, kilichojaa ubani. 69 Alitoa sadaka ya kuteketezwa fahari
mmoja mchanga, dume moja la kondoo, na dume moja la mwanakondoo wa mwaka
mmoja. 70 Alitoa beberu moja kuwa sadaka ya dhambi. 71 Alitoa maksai wawili,
kondoo dume watano, beberu watano, na wanakondoo dume watano wa mwaka
mmoja mmoja, kuwa sadaka ya amani. Hii ndiyo iliyokuwa sadaka ya Ahizeri
mwana wa Amishadai. 72 Siku ya kumi na moja. Pagieli mwana wa Okrani kiongozi
wa uzao wa Asheri alaitoa sadaka yake. 73 Sadaka yake ilikuwa sahani moja ya
fedha yenye uzani wa shekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzani wa shekeli
sabani, kwa kipimo cha shekeli ya mahali patakatifu. Vyombo vyote hivi ilikuwa
vimejaa unga mwembamba uliochanganywa na mafuta kuwa sadaka ya unga. 74 Pia
alitoa kijiko kimoja cha dhahabu chenye uzani wa shekeli kumi, kilichojaa ubani.
75 Alitoa sadaka ya kuteketezwa fahari mmoja mchanga. dume la kondoo moja, dume
moja la mwanakondoo wa mwaka mmoja. 76 Alitoa beberu moja kuwa sadaka ya
dhambi. 77 Alitoa maksai wawili, dume watano wa kondoo, na wanakondoo dume
watano kuwa sadaka ya amani. Hii ndiyo iliyokuwa sadaka ya Pagieli mwana wa
Okrani. 78 Siku ya kumi na mbili., Ahira mwana wa Enani, kiongozi wa uzao wa
Naftali, alitoa sadaka yake. 79 Sadaka yake ailikuwa sahani moja ya fedha yenye
uzani wa shaekeli 130 na bakuli moja la fedha lenye uzani wa shekeli sabini, kwa
kipimo cha shekeli za mahali patakatifu. Vyombo vyote hivi vilikuwa vimejaa unga
mwembamba ulichanganywa na mafuta kuwa sadaka ya unga. 80 Pia alitoa kijiko
kimoja cha dhahabu chenye uzani wa shekeli kumi, kilichojaa ubani. 81 Alitoa sadaka
ya kuteketezwa fahari mmoja mchanga, dume moja la kondoo, na mwanakondoo
dume moja wa mwaka mmoja. 82 Alitoa beberu moja kuwa sadaka ya dhambi.
83 Alitoa maksai wawili, kondoo dume watano, beberu watano, na wanakondoo dume
watano wa mwaka mmoja mmoja kuwa sadaka ya amani. Hii ndiyo iliyokuwa sadaka
ya Ahra mwana wa Enani. 84 Viongozi wa Israeli waliviweka wakfu hivi vitu vyote
siku ambayo Musa alimimina mafuta kwenye madhabahu. Waliziweka wakfu zile
sahani kumi na mbili za fedha, Bakuli kumi na mbili za fedha, na vijiko kumi na
vili vya dhahabu. 85 Zile sahani za fedha kila moja ilikuwa na uzani wa shaekeli 130
na kila bakuli ye fedha ilikuwa na uzani wa shekeli sabini. Vyombo vyote vya fedh

vilikuwa na ujumla ya uzani wa shekeli 2, 400, kwa kipimo cha shekeli za mahali
patakatifu. 86 Vile vijiko vya dhahabu vilivyokuwa vimejaa ubani, vilikuwa na uzani
wa shekeli kumi kila kimoja. Vijiko vyote vya dhahabu vilikuwa na uzani wa shekeli
120. 87 Waliwatenga wanyama wote kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa, fahari kumi
na wawili, kondoo dume kumi na wawili, na wanakondoo dume kumi na wawili wa
mwaka mmoja mmoja. Walitoa sadaka yao ya unga. Walitoa beberu kumi na wawili
kuwa sadaka ya dhambi. 88 Kutokana na ng'ombe zao, walitoa fahari ishirini na nne,
kondoo dume sitini beberu sitini, na wanakondoo dume sitini wa mwaka mmoja
mmoja kuwa sadaka ya amani. Hii ilikuwa kwa ajiliya kuiweka wafu ile madhabahu
baada ya kumiminiwa mafuta. 89 Musa alipoingia kwenye hema ya kukutania kusema
na BWANA, ndipo alipoisikia sauti yake ikisema naye. BWANA alinena naye kutoka
juu ya kiti cha rehema kilichokuwa juu ya sanduku la ushahidi, kutoka katikati ya
makerubi. Alinena naye.

# 8

1 BWANA akanena na Musa, akamwambia, 2 “Sema na Haruni umwambie, 'zile
taa saba lazima zimulike mbele ya kinara utakapoziwasha,” 3 Haruni alifanya haya.
Aliziwasha zile taa juu ya kinara ili ziangaze mbele yake kama BWANA alivyomwa-
giza Musa. 4 Kinara kilitengenezwa kwa njia hii kama BWANA alivyomwelekeza
Musa muundo wake. Kiitakaiwa kutengenezwa kwa dhahabu kuanzia kwenye kitako
chake hadi juu, ndivyo kilivyotakiwa kutengenezwa kwa dhahabu kwa maua hadi
juu. 5 Tena, BWANA akanena na Musa, akasema, 6 '“Uwatwae Walawi kati ya
wana wa Israeli na uwatakase.” 7 Uwafanyie hivi ili kuwatakasa: Uwanyunyizie
maji ya utakaso juu yao. Hakikisha wamenyoa miili yao yote, wafue nguo zao, na
kwa njia hii wajitakase wenyewe. 8 Kisha wachukue fahari mchanga na sadaka ya
unga mwembamba uliochanganywa na mafuta. Halafu wachukue fahari mchanga
kwa ajili ya sadaka ya dhambi. 9 Uwalete Walawi mbele ya hema ya kukutania,
na uwakusanye jamii yote ya wana wa Israeli. 10 Uwalete Walawi mbele yangu,
BWANA. Wana wa Israeli wataweka mikono yao juu ya Walawi. 11 Haruni atawatoa
Walawi mbele yangu, kuwa sadaka ya kutikiswa. Atafanya hivi ili kwamba Walawi
wanitumikie. 12 Walawi wataweka mikono yao juu ya hao fahari. Mtatoa fahari
mmoja kuwa sadaka ya dhambi na fahari mwingine kuwa sadaka ya kuteketezwa
kwangu, ili kuwa upatanisho kwa Walawi. 13 Walete Walawi mbele ya Haruni na
mbele ya wana wake, uwainue kuwa sadaka ya kutikiswa kwa ajili yangu. 14 Kwa
njia hii utawatenganisha Walawi toka wana wa Israeli. Walawi watakuwa wangu.
15 Baadaye Walawi wataingia ndani ya hema ya kukutania. Utawatakasa. utawatoa
kuwa sadaka ya kutikiswa 16 Fanya hivi kwa sababu wao ni wangu wote kutoka
kwa wana wa Israeli. Watachukua nafasi ya kila mzaliwa wa kwanza afunguaye
tumbo, mzaliwa wa kwanza wa uzao wa Israeli. Nimewachukua Walawi kwa ajili
yangu. 17 Wazaliwa wa kwanza wote kutoka kwa wana wa Israeli ni wangu, watu
wote pamoja na wanyama pia. Siku ile nilipowachukua wazaliwa wa kwanza katika
nchi ya Misri, Niliwatenga kwa ajili yangu 18 Nimewachukua Walawi kutoka kwa
wana wa Israeli badala ya wazaliwa wa kwanza. 19 Nimewatoa Walawi kuwa zawadi
kwa Haruni na wana wake. Nimewachukua toka wana wa Isreali ili kuwatumikia
wana wa Israeli katika hema ya kukutania. Nimewatoa ili kuwa upatanisho kwa
watu ili kwamba wasipatwe na mapigo wakati wanapokaribia kwenye eneo takatifu.
20 Musa, Haruni na jamii ya Waisraeli wote waliwafanyia Walawi hivi. Walifanya kila
kitu ambacho BWANA alikuwa amemwamuru Musa kuhusu Walawi. Wana wa Israeli
wakafanya haya pamoja nao. 21 Walawi wakajitakasa wenyewe na kufua mavazi yao,
Na Haruni akawatoa kama sadaka ya kutikiswa kwa BWANA na akafanya upatanisho

kwao ili kuwatakasa. [22] Baada ya hayo, Walawi waliingia ndani kufanya utumishi
wao katika hema ya kukutania mbele ya Haruni na mbele ya wanawe. Kama BWANA
alivyokuwa amemwagiza Musa juu ya Walawi. Waliwahudumia Walawi wote kwa
jinsi hii. [23] BWANA akanena na Musa tena, Akasema, [24] "Haya yote ni kwa ajili ya
Walawi ambao wana umri wa miaka ishirini na mitano na zaidi. Wataungana na
wale wanaohudumia hekaluni. [25] Wataacha kutoa huduma hii watakapokuwa na
umri wa miaka hamsini. Katika umri huu hawatakiwi kuendelea na huduma tena.
[26] Wanaweza kuwasaidia ndugu zao wanaoendelea kufanya kazi ndani ya hema ya
kukutania, lakini hawatakiwai kufanya kazi tena. Utawaelekeza Walawi kuyafahamu
haya yote."

# 9

[1] BWANA akanena na Musa katika katika jangwa la Sinai, mwezi wa kwanza wa
mwaka wa pili baada ya kutoka katika nci ya Misri. Akasema, [2] "Wana wa Israeli
wataikumbuka Pasaka katika wakati wake kila mwaka. [3] Siku ya kumi na nne ya
mwezi huu, muda wa jioni, utaikumbuka Pasaka kila mwaka kwa muda uliopanggwa.
Lazima uikumbuke, fuata taratibu zake zote na utii sheria zake zote zinazohusiana na
tukio hilo. [4] Kwa hiyo, Musa akawaambia wana wa Isareli kuwa wataishika sikukuu
ya Pasaka. [5] Kwa hiyo wakaishika sikuu ya Pasaka katika mwezi wa kwanza, wakati
wa jioni wa siku ya kumi na nne ya mwezi katika jangwa la Sinai. Wana wa Israeli
walitii kila kitu ambacho BWANA alimwamuru Musa kukifanya. [6] Kulikuwa na watu
fulani walionajisika kwa sababu ya maiti ya mtu. Hawakuweza kuishika Pasaka siku
hiyo. Kwa hiyo walikwenda kwa Musa na Haruni siku hiyohiyo. [7] Wakamwambia
Musa, "Sisi tumenajisika kwa sababu ya maiti ya mtu. Kwa nini basi unatutaka
tuendelee kutoa sadaka kwa BWANA kwa wakati wa mwaka uliopangwa kwa wana
wa Israeli?" [8] Naye Musa akawaambia, "Subirini nimsikilize BWANA ataniambia nini
juu Yenu." [9] BWANA akanena na Musa, akamwambia, [10] "Nena na wana wa Israeli,
uwaambie, 'kama mmoja wenu au mwana wa uzao wenu amenajisika kwa sababu ya
maiti, au ana safari ndefu, bado anaweza kuishika Pasaka ya BWANA. [11] Wataishika
Pasaka siku ya kumi na nne ya mwezi wa pili wakati wa jioni. Wataila kwa mikate
isyotiwa chahcu na mboga chungu. [12] Wasiiache mpaka jioni, au kuvunja mifupa
yake. Watafuata taratibu zote za Pasaka. [13] Lakini mtu yeyote asiye najisi na hayuko
safarini, na akashindwa kuishika Pasaka, huyo mtu lazima aondolewe kati ya watu
wake kwa sababu hakutoa sadaka ambayo BWANA huitaka kwa wakati wa mwaka
uliopangwa. Huyo mtu lazima aibebe dhambi yake. [14] Kama mtu mgeni anayeishi
kati yenu na akaishika, Pasaka kwa heshima ya BWANA, ataishika na kufanya amri
zote, na kutii taratibu zake. Utakuwa na sheria hizohizo kwa wageni na kwa wote
waliaozaliwa katika nchi. [15] Na siku hiyo ambayo masikani iliposimamishwa, wingu
lilifunika masikani, ile hema ya amari ya agano. Ilipokuwa jioni wingu lilkuwa juu
ya masikani. Lilionekana kama moto mpaka asubuhi. [16] Liliendelea hivyohivyo. Lile
wingu lilifunika masikani na kuonekana kama moto wakati wa usiku. [17] Na kila
wingu lilipochukuliwa kutoka kwenye hema, wana wa Isareli waliendelea na safari
yao. Na kila wingu liliposimama, watu waliweka kambi. [18] Wana wa Israrli walisafiri
kwa amri ya BWANA, na kwa amri yake waliweka kambi. Wakati wingu liliposimama
juu ya masikani, nao walikaa kwenye kambi zao. [19] Na wingu lilipobaki kwenye
masikani kwa siku nyingi, wana wa Israeli walitakiwa kutii maelekezo ya BWANA na
kusitisha safari yao. [20] Wakati mwingine wingu lilibaki kwa siku chache tu kwenye
masikani. Kwa mazingira kama hayo walilazimika kutii amri ya BWANA - waliweka
kambi na kisha kuendelea na safari tena kwa amri yake. [21] Wakati mwingine
wingu lilikuwepo kambini kuanzia jioni mpaka asubuhi. Na wingu liliponyanyuliwa

asubuhi, walisafiri. Kama liliendelea kwa mchana wote na kwa usiku wote, ni pale tu
wingu liliponyanyuliwa ndipo walipoendelea na safari. 22 Hata kama wingu lilibaki
kwenye masikini kwa siku mbili, kwa mwezi mmoja, au kwa mwaka mmoja, ili mradi
tu limebaki pale, wana wa Israeli walibaki kwenye kambi zao na kusitisha safari.
Lakini pale wingu liliponyanyuliwa, walianza safari yao. 23 Walifanya kambi kwa
amri ya BWANA, na walisafiri kwa amri yake. Walitii amri ya BWANA iliyotolewa
kupitia kwa Musa

# 10

1 BWANA alinena na Musa, akasema, 2 "tengenza tarumbeta mbili za fedha.
Uzitengeneze kwa kufua hizo fedha. Utazitumia hizo tarumbeta kwa kuwaita watu
waje pamoja na kwa kuwaita watu wote wakati wa kuondoka kwenye kambi zao.
3 Makuhani watapiga tarumbeta kwa ajili ya kuwaita watu wote mbele yako kwenye
lango la hema ya kukutania. 4 Kama makuhani watapiga tarumbeta moja tu,
basi viongozi, vichwa koo za Israeli ndipo watakapokutana kwako. 5 Utakapopiga
tarumbeta ya sauti kuu, ile kambi ya upande wa mashariki itaanza kusafiri. 6 Nawe
utakapopiga tarumeta kwa sauti kuu mara ya pili, ile kambi ya upande wa kusini
wataanza kusafiri. Watapiga tarumbeta kwa sauti kuu ili kuanza safari yao. 7 Watu
wote watakapokutana pamoja, piga hizo tarumbeta lakini si kwa sauti kuu. 8 Wana
wa Haruni, makuhani, watapiga hizo tarumbeta. Huu ndio utakaokuwa utaratibu
wa watu wako kwa vizazi vyote. 9 Nanyi mtakapoenda vitani katika ardhi yenu
dhidi ya maadui wenu wanaowakandamiza, ndipo mtakapotoa ishara ya sauti ya
tarumbeta. Mimi, BWANA Mungu wako nitawaita kuwakumbuka na kuwaokoa
kutoka kwa maadui wenu. 10 Pia, wakati wa kusherehekea, sikukuu zenu za kawaida
na katika miandamo ya miezi, mtapiga tarumbeta zenu kwa heshima ya sadaka
zenu za kuteketezwa na kwa sadaka zenu za amani. Huu utakuwa ukumbusho
wenu kwangu, Mungu wenu. Mimi ndimi BWANA Mungu wenu." 11 Katika siku ya
ishrini, mwezi wa pili, mwaka wa pili, Lile wingu liliinuliwa toka masikani ya amri
za maagano. 12 Wana wa Israeli wakaendelea na safari yao toka jangwa la Sinai.
Lile wingu likasimama kwenye jangwa la Parani. 13 Walifanya safari yao ya kwanza,
kufuatia amri ya BWANA iliyotolewa kupitia kwa Musa. 14 Kambi ya mahali pa uzao
wa Yuda iliondoka ya kanza, wakiondoa majeshi yao binafsi. Nashoni mwana wa
Aminadabu ndiye aliyeongoza jeshi la Yuda. 15 Nethaneli mwana wa Zuari aliongoza
jeshi la kabila la uzao wa Isakari. 16 Eliabu mwana wa Heloni aliongoza jeshi la
kabila la Zabuloni. 17 Uzao wa Gerishoni na Merari, ambao walitunza masikani,
na kuanza kusafiri. 18 Baadaye Walifuata jeshi la mahali pa kambi ya Reubeni
walianza safari yao. Elizuri mwana wa Shedeuri alliongoza jeshi la Reubebni.
19 Shelumieli mwana wa Zurishadai aliliongoza jeshi la kabila la uzao wa Simeoni.
20 Eliasafu mwana Deuli aliliongoza jeshi la kabila la uzao wa Gadi. 21 Kabila la
Kohathi nalo lilianza safari. Wao walibebba vyombo vya mahali patakatifu. Wengine
waliisimamisha masikani kabla ya Wakohathi kufika kambi inayofuata. 22 Majeshi
ya kabila la uzao wa Efraimu ndio waliofuata. Elishama mwana wa Amihudi ndiye
aliyeongoza jeshi la Efraimu. 23 Gamalieli mwana wa Pedazuri aliongoza jeshi la
uzao wa Manase. 24 Abidani mwana wa Gidioni aliongoza jeshi la uzao wa kabila la
Benjamini. 25 Lile jeshi lililoweka kambi mahali pa bango la uzao wa Dani lilikuwa
la mwisho kuondoka. Ahizeri mwana wa Amishadai ndiye aliyeongoza jeshi la Dani.
26 Pagieli mwana wa Okirani aliongoza jeshi la wana wa uzao wa Asheri. 27 Ahira
mwana wa Enani aliongoza jeshi la uzao wa kabila ya Naftali. 28 Hivi ndivyo majeshi
ya wana wa Israeli yalivyosafiri. 29 Musa alinena na Hobibu mwana wa Reueli wa
Kabila la Midiani. Reueli alikuwa baba mke wa Musa. Musa akanena na Hobibu

akasema, “Tunasafiri kuelekea mahali ambapo BWANA ametuahidi. BWANA alisema
kuwa, “Nitawapeni ninyi hilo eneo, 'Njoni pamoja nasi na tutawatendea mema.
BWANA ameahidi kuwafanyia mema Waisraeli.” 30 Lakini Hobibu akmwambia Musa,
“Sitaambatana nanyi.” 31 Naye Musa akamjibu, “Tafadhali msituache. Mnajua jinsi
ilivyo kuweka kambi jangwani. Tunaomba mtujali. 32 Kama mtaambatana nasi
tutawatendea mema sawa na jinsi BWANA anavyotutendea.” 33 Walisafiri kutoka
mlima wa BWANA kwa siku tatu. Sanduku la agano la BWANA liliwatangulia kwa
siku tatu ili kupata mahali pa kupumzika. 34 Wingu la BWANA lilikuwa juu yao
muda wote wa mchana walipokuwa safarini. 35 Kila hilo sanduku liliposafiri kwenda
mbele, Musa alisema, “Inuka BWANA, Uwatawanye maadui wako. Uwafanye wale
wanaokuchukia kukukimbia.” 36 Na kila lile sanduku liliposimama, Musa alisema,
“BWANA uwarudie, hawa Waisraeli makumi elfu.”

# 11

1 Sasa watu wakanung'unika juu ya matatizo yao wakati BWANA alipokuwa
akiwasikiliza. BWANA akawasikia watu naye akakasirika. Moto kutoka kwa BWANA
ukashuka na ukawaka kati yao na kuteketeza baadhi ya kambi kwenye pembe zake.
2 Ndipo watu wakamwita Musa kwa nguvu, Naye Musa akamwomba BWANA, na
ule moto ukazimika. 3 Mahali pale paliitwa Tabera, kwa sababu moto wa BWANA
uliwaka kati yao. 4 Baadhi ya wageni wakaanza kuweka kambi zao pamoja na wana
wa wa Israeli. Walitaka kula chakula kizuri. Kisha wana wa Israeli walipoanza
kulia wakisema, “Ni nani atakayetupatia nyama za kula? 5 Tunakumbuka samaki
tulizokula bure kule Misri, yale matango, na matikiti maji, na mboga na vitunguu
na vitunguu saumu. 6 Na sasa hatuna hamu ya kula, kwa sababu tunaona mana tu.
7 Mana ilifanana na punje ya mtama. ilionekana kama bedola. 8 watu wakazunguka
kisha wakakusanyika. Wakaisaga, wakaitwanga kwa vinu, wakaitokosa nyunguni,
na kuitengeneza mikate. radha yake ilikuwa kama mafuta mapya ya mizeituni. 9 Na
umande ulipoanguka kambini usiku ule, na mana ilianguka pia. 10 Musa akawasikia
watu wakilia katika familia zao, na kila mtu alikuwa kwenye lango la hema yake.
BWANA alikasirika sana, na mbele ya macho ya Musa malalamiko yao yalikuwa
mabaya. 11 Musa akasema na BWANA, “Kwa nini umemtendea mtumishi wako
vibaya namna hiyo? kwa nini hujapendezwa na mimi? unanifanya kubeba mizigo
ya hawa watu. 12 Je, mimi ndiye niliyewatungia mimba hawa watu? Mimi ndiye
niliyewazaa kiasi kwamba unaniambia, “wabebe kwa ukaribu vifuani mwako kama
baba abebavyo mtoto wake? Je, nitawabeba mpaka kwenye nchi ambayo uliwaahidi
mababu zao kuwapa? 13 Naweza kupata wapi nyama za kuwapa watu wote hawa?
Wanalia mbele zangu na wanasema, 'tupe nyama tule.' 14 Mimi peke yangu siwezi
kuwabeba watu wote hawa. Ni wengi sana kwangu. 15 Kwa vile unanitendea hivi,
basi uniue, na kama wewe ni mpole kwangu, basi niondolee mzigo huu.” 16 BWANA
akamwambia Musa, “Niletee wazee sabini miongoni mwa Waisraeli. Hakikisha ni
wazee na viongozi wa watu. Uwalete kwenye hema ya kukutania wasimame pamoja
na wewe. 17 Nami nitashuka niseme nawe mahali pale. Nitatoa sehemu ya roho
iliyo ndani yako na kuwapatia wao. Nao watabeba mzigo wa watu pamoja nawe. na
hautaubeba peke yako. 18 Waambie watu, 'Jitakaseni ninyi wenyewe, kwa kuwa kesho
mtakuala nyama, kwa kuwa mmelia na BWANA amesikia, “Mlipokuwa mkisema
kuwa nani atakayetupa nyama tule? Kule Misri tulikula chakula kizuri!” Kwa hiyo
BWANA atawapeni nyama, nanyi mtakula nyama. 19 Hamtakula nyama kwa siku
moja tu, au siku mbili, au siku tano, au siku kumi, au siku ishirini, 20 Lakini mtakula
nyama kwa mwezi mmoja mpaka zitakapowatokea puani. Mpaka zitawakinai kwa
sababu mmemkataa BWANA ambaye yuko kati yenu. Mmelia mbele yake. mmesema,

“Kwa nini tulitoka Misri?”” [21] Kisha Musa akasema, “Mimi nina watu 600, 000, na
wewe umesema, “Nitawapa nyama mle kwa mwezi mmoja,' [22] Je, tutayachinja haya
makundi ya ng'ombe na kondoo ili kuwatosheleza?” [23] BWANA akasema na Musa,
“Je mkono wangu ni mfupi? Sasa utaona kama maneno yangu ni ya kweli ama sivyo.
[24] Musa alitoka nje kwenda kuwaambia watu maneno ya BWANA. Aliwakusanya
wazee sabini wa watu na kuwaweka kuizunguka hema. [25] BWANA akashuka chini
katika wingu akaongea na Musa. BWANA akachukua sehemu ya roho iliyokuwa
kwa Musa na kuiweka kwa wale wazee sabini. Roho alipowashukia, wakaanza
kutoa unabii, lakini ilitokea kwenye tukio hilo tu na haikujirudia tena. [26] Watu
wawili waitwao Elidadi na Medadi walibaki kambini. Lakini Roho aliwashukia pia.
Majina yao yalikuwa yameandikwa kwenye orodha lakini walikuwa hawajaenda
hemani. Hata hivyo nao walitoa unabii wakiwa kambini. [27] Kijana mmoja huko
kambini alikimbia akaenda kumwambia Musa, “Elidadi na Medadi wanatoa unabii
kambini.” [28] Joshua mwana wa Nuni, msaidizi wa Musa, ambaye ni miongoni mwa
wale aliowachagua akamwambia Musa, “Bwana wangu Musa, wazuie.” [29] Musa
akamwambia, “una wivu kwa niaba yangu? Natamani kama watu wote wa BWANA
wangekuwa manabii na kwamba angeweka Roho yake juu yao wote!” [30] Kisha Musa
na wale wazee wakarudi kambini. [31] Kisha upepo ukavuma kutoka kwa BWANA
ukaja na kware kutokea baharini. Wakaanguka karibu na kambi, kiasi cha umbali
wa safari ya siku moja upande huu na umbali wa siku moja upande mwingine.
Wale kware wakaizunguka kambi kiasi cha mita moja toka uso wa dunia. [32] Watu
wakawakusanya hao kware kwa bidii mchana huo wote na usiku huo wote, na
mchana wote uliofuatia. Hakuna aliyekusanya pungufu ya mita mbili za uajazo.
Wakawaanika kweye ardhi yote hapo kambini. [33] Wakati ile nyama ikiwa bado iko
kwenye meno yao, wakiwa bado wanatafuna, BWANA akawakasirikia. Akwapiga
watu wale kwa gonjwa kubwa sana. [34] Mahali pale paliitwa Kibroti Hataava, kwa
sababu pale walizika watu waliotamani nyama. [35] Kutoka Kibroti Hataava watu
wakasafiri hadi Hazeroti, ambapo walipumzika.

# 12

[1] Kisha Miriamu na Haruni wakasema kinyume na Musa kwa sababu ya
mwanamke Mkushi ambaye alikuwa amemwoa. [2] Walisema. “ Hivi BWANA amesema
na Musa tu? Ni kweli hajawahi kusema nasi pia? Sasa BWANA akasikia kile
walichokuwa wanaongea. Sasa [3] Musa alikuwa mtu mpole sana, mpole kuliko mtu
yeyote duniani. [4] Wakati huo, BWANA akanena na Musa, Haruni na Miriamu: “tokeni
nje ninyi watatu kwenye hema ya kukutania.” kwa hiyo wale watatu wakatokanje.
[5] Kisha BWANA akashuka katika nguzo ya wingu. Akasimama kwenye lango la hema
na akamwita Haruni na Miriamu. wote wakaja mbele. [6] BWANA akasema, “Sasa
sikilizeni maneo yangu, Nabii wangu anapokuwa nanyi, Mimi nitajifunua kwake
kwa maono na kusema naye katika ndoto. [7] Lakini si hivyo kwa mtumishi wangu
Musa. Yeye ni mwaminifu katika nyumba yangu yote. [8] Mimi huongea na Musa
moja kwa moja, si kwa maono wala mafumbo. Yeye huniona umbo langu. Kwa
hiyo, kwa nini hamuogoopi kumnenea kinyume, mtumishi wangu Musa?” [9] Hasira ya
BWANA ikawawakia, kisha akawaacha. [10] Lile wingu likainuka juu ya hema, Miriamu
akapata ukoma ghafla - akawa mweupe kama theluji. Naye Haruni alipogeuka
kumwona Miriamu, akamwona amepata ukoma. [11] Haruni akamwambia Musa,
“Bwana wangu, usituadhibu kwa uovu wetu huu. Tumenena katka upumbuvu, na
tumetenda dhambi. [12] Tafadhali nakuomba usimwache akawa kama mtoto mchanga
aliyekufa ambaye nusu ya nyama yake imeoza tangu kuzaliwa” [13] Kwa hiyo Musa
akamwomba BWANA, akasema, “Mungu ninakusihi umponye tafadhali.” [14] BWANA

akamwambia Musa, “ kama baba yake angemtemea usoni angepata aibu kwa muda
wa siku saba. Umfungie nje ya kambi kwa muda wa siku saba. Kisha umrejeshe
ndani tena.” 15 Kwa hiyo Miriamu akafungiwa nje ya kambi kwa siku saba. Watu
hawakusafiri mpaka aliporudi kambini. 16 Kisha watu wakasafiri kutoka Hazeroti na
kuweka kambi kwenye jangwa la Parani.

# 13

1 Kisha BWANA akanena na Musa, akamwambia, “tuma watu waende kuipeleleza
nchi ya Kanani, ambayo nimewapa wana wa Israeli. 2 Tuma mwanamume mmoja
kutoka kila jamaa ya kabila. Kila mwanamume awe kiongozi katika kabila lake.”
3 Musa akawatuma kutoka jangwa la Parani, ili watii amri ya BWANA. Watu wote
hao walikuwa viongozi wa watu wa Israeli. 4 Majina yao yalikuwa haya yafuatayo:
kutoka kabila la Reubeni, Shamua mwana wa Zakuri; 5 Kutoka kabila la Simeoni,
Shafati mwana wa Hori; 6 Kutoka kabila la Yuda, Kalebu mwana wa Yefune; 7 Kutoka
kabila la Isakari, Igali mwana wa Yusufu, 8 Kutoka kabila la Efraimu, Hoshea mwana
wa Nuni; 9 Kutoka kabila la Benjamini, Paliti mwana wa Rafu; 10 kutoka kabila ya
Zabuloni, Gadieli mwana wa Sodi; 11 kutoka kabila la Yusufu (hiyo inamaanisha
kutoka kabila la Manase), Gadi mwana wa Susi; 12 kutoka kabila la Dani, Amieli
mwana wa Gemalili; 13 kutoka kabila Asheri, Setu mwana wa Mikaili; 14 kutoka
kabila la Naftali, Nabi mwana wa Vofisi; 15 kutoka kabila la Gadi, Geuli mwana
wa Machi. 16 Haya ndiyo majina ya wanaume ambao Musa aliwatuma kwenda
kuipelelza ile nchi. Musa akamwita Hoshea mwana wa Nuni kwa jina la Joshua.
17 Musa akawatuma kwenda kuipeleleza ile nchi ya Kanani. Naye akawaambia, “
Mkaanzie Negebu hadi mahali pa milima. 18 Kaipelelezeni nchi kujua ni nchi ya
namna gani. Wachunguzeni watu wake, kama ni watu wenye nguvu au dhaifu,
kama ni wachache au ni wengi. 19 Chunguzeni nchi hiyo wanayoishi ni nchi ya
namna gani. Ni nzuri au mbaya? Miji yao ikoje? Je iko kama kambi au ni miji
yenye ngome? 20 Chunguzeni ni nchi ya namna gani, kama ni njema kwa mazao
au la kama kuna miti au hapana. Mwe hodari mkalete sampuli za mazao ya nchi,”
Sasa ni muda wa msimu wa malimbuko ya mizabibu. 21 Kwa hiyo wale wanaume
wakaenda kuipeleleza ile nchi kutoka jangwa la Sini mpaka Rehobi, karibu na Lebo
Hamati. 22 Walienda kutoka Negebu nao wakafika Hebroni. Ahimani, Sheshai, na
Talmai, Uzao wa Anaki nao walikuweko, Sasa Hebroni ilikuwa imejengwa miaka
saba iliyokuwa imepita kabla ya Zoani wa Misri. 23 Nao walipofika katika bonde
la Eshikoli, walikata matawi ya mizabibu lenye kishada cha zabibu. Na makundi
mawili ya wapelelezi wakakibeba kwenye mti. Pia wakaleta makomamanga na mtini.
24 Mahali pale paliitwa Eshikoli, kwa sababu ya kishada cha mizabibu ambacho wana
wa Israeli walikata kule. 25 Baada ya siku arobaini, wakarudi kutoka kuipeleleza
nchi. 26 Wakaja kwa Musa, Haruni na kwa watu wote wa Israeli katka jangwa la
Parani, kule Kadeshi. Wakaleta taarifa kwao na kwa Waisraeli wote, na kuwaonyesha
matunda ya nchi ile. 27 Wakamwambia Musa, “Tulifika katika ile nchi uliyotutuma.
Kwa hakika ni nchi ya kutiririka maziwa na asali. Na baadhi ya matunda yake ni
haya hapa. 28 Hata hivyo, watu wanaoishi huko ni wenye nguvu. Miji yao ni mikubwa
tena ina maboma. Pia tuliwaona wana wa Anaki huko. 29 Waamaleki wanaishi
Negebu. Wahiti, Wayebusi, na Waamori nao wanaishi katika milima ya hiyo nchi.
Wakanaani wanaishi kando ya bahari na mto Yorodani.” 30 Kisha Kalebu akawatuliza
watu waliokuwa mbele ya Musa, akasema, “Twendeni tukaiteke nyara hiyo nchi,
kwa kuwa tuna uhakika wa kuikamata.” 31 Lakini wale watu waliokuwa wameenda
naye walisema, “Hatutaweza kuwashinda hao watu kwa kuwa wao ni hodari kuliko
sisi.” 32 Kwa hiyo wakasambaza taarifa za kukatisha tamaa kwa Wana wa Israeli juu
ya nchi ile waliyoipeleleza. Walisema, “Ile nchi tuliyoiona ni nchi inayowala watu

wake. Watu wote tuliowaona ni watu warefu. 33 Kule tuliiona majitu, wana wa uzao
wa Anaki, ambao nii uzao wa majitu. Sisi tulionekana kama panzi machoni mwao
tulipojilingsnisha nao, hivyo ndivyo tulivyoonekana machoni mwao pia."

# 14

1 Usiku huo watu wote walilia kwa sauti. 2 Watu wote wa Israeli wakamlalamikia
Musa na Haruni. Watu wote wakawaambia, "Ni bora kama tungelifia katika nchi ya
Misri, au katika hili! 3 Kwa nini BWANA alituleta katika nchi hii ili tufe kwa upanga?
Wake zetu na watoto wetu watakuwa watumwa wao. Je, si bora kwetu kurudi
Misri?" 4 Wakasemezana wao kwa wao, "Na tuchague kiongozi mwingine, turudi
Misri." 5 Ndipo Musa na Haruni wakalala kifudifudi mbele ya kundi lote la wana
wa Israeli. 6 Joshua mwana wa Nuni na Kalebu mwana wa Yefune, ambao walikuwa
miongoni mwa wale waliokuwa waemtumwa kwenda kuipeleleza nchi wakachana
mavazi yao. 7 Wakawaambia watu wote wa Israeli. Walisema, "Ile nchi tuliyopita
katikati yake ni nchi nzuri sana. 8 Kama BWANA amependezwa nasi, basi atatuingiza
katika nchi hii na kutupatia. Ile nchi inatiririka maziwa na asali. 9 Lakini msimwasi
BWANA, na msiwahofie hao wakazi wa nchi hiyo. Tutawateketeza kwa urahisi kama
kula chakula. Ulinzi wao utaondolewa kutoka kwao, kwa sababu BWANA yuko
pamoja nasi. Msiwahofie." 10 Lakini watu wote walitishia kuwapiga kwa mawe
mpaka wafe. Kisha utukufuwa BWANA ukaonekana kwenye hema ya kukutania
kwa watu wote wa Israeli. 11 BWANA akamwambi Musa, "watu hawa watanidharau
hadi lini? Wataendelea kutoniamini mpaka lini? Nijapokuwa nimefanya ishara
kwa nguvu zangu kati yao? 12 Nitawapiga kwa mapigo, na kuwaondolea urithi, na
kufanya taifa kubwa kutoka kwenye ukoo wako ambalo litakuwa kubwa na lenye
nguvu kuliko wao. 13 Musa akamwambia BWANA, "Kama utafanya hivi, Na Wamisiri
wakisikia habari hizi, na kwa sababu uliwaokoa kutoka kwao kwa nguvu zako. 14 Basi
watawaambia wakazi wa nchi hii. Wamesikia ya kuwa wewe BWANA u kati ya watu
hawa, kwa sababu uso wako waonekana. Wingu lako husimama juu ya watu wetu.
Wewe huwatangulia katika nguzo ya wingu wakati wa mchana na katika nguzo ya
moto wakati wa usiku. 15 Sasa kama utawaua hawa watu kama mtu mmoja, basi
mataifa ambao wamesikia sifa zako watasema, 16 "Kwa Sababu BWANA hana uwezo
wa kuwapeleka watu hawa katika nchi ambayo aliwaapia kuwapa, ndiyo maana
amewaua katika jangwa hili.' 17 Sasa, nakusihi, utumie uweza wako. Kwa kuwa
umesema kuwa, 18 'BWANA si mwepesi wa hasira na ni mwingi wa uaminifu katika
agano. Yeye husamehe uovu na uasi. Kwa vyovyote vile atafutilia hatia atakapoleta
hukumu ya dhambi za mababu juu ya wazao wao, kwa kizazi cha tatu na cha
nne.' 19 Ninakusihi uwasameha watu hawa dhambi zao kwa sababu ya ukuu wa
uaminifu wa agano lako, kama vile ambavyo umekuwa ukiwasamehe watu hawa
tokea wakati wakiwa Misri mpaka sasa." 20 BWANA akasema, Nimewasamehe kwa
kama ulivyoomba, 21 bali kama Niishivyo, na kama vile dunia yote itakavyojazwa na
utukufu wangu, 22 watu wote walioona utukufu wangu na ishara za nguvu zangu
nilizotenda kule Misri na kule jangwani - Lakini bado wamenijaribu mara kumi sasa
na hawakuisikiliza sauti yangu. 23 Kwa hiyo nasema kwamba hakika hawataiona
nchi ile ambayo niliwaahdi kuwapa mababu zao. Hakuna hata mmoja wao ambao
wamenidharau watakaoiona, 24 isipokuwa mtumishi wangu Kalebu, kwa sababu
alikuwa na roho nyingine. Yeye amenifuata kwa ukamilifu; Yeye nitampeleka katika
nchi hiyo ambayo alienda kuipeleleza. Wazao wake wataimilki. 25 (Sasa Waamaleki
na Wakanani waliishi katika bonde.) Kesho mtageuka na kwenda katika jangwa
kwa njia ya bahari ya Shamu." 26 BWANA akanena na Musa na Haruni, akasema,
27 "Nitaivumilia jamii ya watu hawa waovu ambao wananinung'unikia mpaka lini?

Nimeyasikia malalamiko ya wana wa Israeli dhidi yangu. 28 Waambie, 'Kama
niishivyo,' asema BWANA, 'kama vile mlivyosema katika masikio yake, nitawafanyia
jambo hili: 29 Maiti zenu zitaanguka katika jangwa hili, Ninyi nyote mliolalamika
dhidi yangu, ninyi mliohesabiwa kwenye ile sensa, idadi yote ya watu kuanzia umri
wa mika ishirini na kuendelea. 30 Kwa hakika hamtaingia kwenye ile nchi ambayo
niliahidi kuwapa kuwa makazi yenu, isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune na Joshua
mwana wa Nuni. 31 Bali watoto wenu ambao mlisema kuwa watakuwa watumwa,
wao ndio nitakaowapeleka katika nchi hiyo. Wao wataifurahia nchi ambayo nInyi
mmeikataa! 32 Lakini ninyi, maiti zenu zitaanguka katika jangwa hili. 33 Watoto wenu
watakuwa wachungaji katika jangwa hili kwa muda wa miaka arobaini. Lazima
watabeba madhara ya matendo yenu ya kutokuamini mpaka mwisho wa maiti ya
mwisho jangwani. 34 Kama vile ilivyo hesabu ya siku ambayo mliipeleleza nchi—
siku arobaini, vivyo hivyo mtabeba madhara ya dhambi zenu kwa muda wa miaka
arobaini—mwaka mmoja kwa kila siku moja, na mtajua kuwa ni sawa na kuwa
adui yangu. 35 Mimi BWANA nimesema. Hakika nitafanya hivi kwa kizazi hiki
chote kiovu ambacho kimekusanyika kinyume na Mimi. Wao watakatwa kabisa,
na watafia hapa.'" 36 Kwa hiyo wale wanaume ambao Musa aliwatuma kwenda
kuingalia ile nchi wote walikufa kwa tauni mbele ya BWANA. 37 Hawa ni wale
ambao waliorudi na kutoa taarifa mbaya juu ya nchi. Hii iliwafanya watu wote
wamlalamikie Musa. 38 Kati ya watu wale waliokuwa wameenda kuiangalia nchi
ile, ni Joshua mwana wa Nuni na Kalebu mwana wa Yefune tu ndio waliobaki
hai. 39 Musa alipowataarifu mambo haya watu wote wa Israeli waliomboleza sana.
40 Waliamka asubuhi na mapema wakaenda juu ya mlima na kisha wakasema,
"Tazama, tuko hapa, na tutaenda mahali pale ambapo BWANA ametuahidi, kwa
kuwa tumetenda dhambi." 41 Lakini Musa akasema, "Kwa nini sasa mnapinga amri
ya BWANA? hamtafanikiwa. 42 Msiende, kwa sababu BWANA hayuko pamoja nanyi
kuwalinda dhidi ya maadui zenu. 43 Waamaleki na Wakanaani wako kule, na mtakufa
kwa upanga kwa sababu mliumtegea mgongo BWANA na hamkumfuata. Kwa hiyo
hatakuwa pamoja nanyi. 44 Lakini walithubutu kukwea mlimani; lakini si Musa wala
Sanduku la agano la BWANA walioondoka kambini. 45 Kisha Waamaleki walikuja
chini, pia wale Wakanaani walioshi kwenye hiyo milima. Wakawavamia Waisreli
wakawapiga na kuwaangusha mpaka Horima.

# 15

1 Kisha BWANA akanena na Musa, akasema, 2 "Sema na wana wa Israeli uwaambie,
'Mtakapoingia katka nchi ambayo mtaishi, ambayo BWANA atawapa, 3 mtatakiwa
kuandaa sadaka kwa moto kwa BWANA, sadaka ya kuteketezwa au sadaka ya
kukamilisha kiapo au sadaka ya hiari, au sadaka katika sikukuu zenu, ili kutoa
harufu nzuri kwa BWANA ya ng'ombe au ya kondoo. 4 Utamtolea BWANA sadaka
ya kuteketezwa pamoja na sehemu ya kumi ya efa ya sadaka ya unga mwembamba
uliochanganywa na robo ya hini ya mafuta. 5 Na tena mtatoa pamoja na sadaka
ya kuteketezwa, au kwa sadaka ya divai robo ya hini ya sadaka ya vinywaji kwa
kila mwanakondoo. 6 Kama unatoa sadaka ya kondoo dume, utaandaa sadaka ya
unga ya sehemu za kumi mbili za efa ya unga mwembamba uliochanganywa na
sehemu ya tatu ya hini ya divai. 7 Kwa sadaka ya kinywaji, mtatoa sehemu ya
tatu ya hini ya divai ambayo itatoa harufu nzuri kwa BWANA. 8 Utakapoandaa
fahari kwa ajiliy a sadaka ya kuteketezwa au sadaka ya kutimiza kiapo, au sadaka
ya amani kwa BWANA, 9 Ndipo utakapotoa sadaka ya fahari pamoja na sadaka
ya unga ya sehemu za kumi tatu za unga mwembamba uliochanganywa na nusu
ya hini ya mafuta. 10 Mtatoa sadaka ya kinywaji nusu ya hini ya divai, sadaka

iloyotengenezwa kwa moto ili kufanya harufu nzuri kwa BWANA. 11 Itafanyika hivi
kwa kila fahari, kwa kila kondoo dume, na kila mwanakondoo dume au mbuzi
mchanga. 12 Kila sdaka utakayoindaa na kuitoa itafanyika kama ilivyoanishwa
hapa. 13 Wazawa wote wa Israeli watafanya mambo haya kwa utaratibu huu, yeyote
atakayeleta sadaka iliyotengenezwa kwa moto, ili kufanya harufu nzuri kwa BWANA.
14 Na kama kuna mgeni anayeishi kati yenu, au yeyote atakayeishi na watu wa
vizazi vyenu vyote, lazima atengeneze sadaka iliytoengenezwa kwa moto, ili kutoa
harufu nzuri kwa BWANA. Atafanya kama mnavyofanya. 15 Kutakuwa na sheria
hiyo hiyo kwa watu wote na kwa mgeni anayeishi kati yenu, sheria ya kudumu kwa
watu wote wa uzao wako. Ninyi mlivyo, ndivyo atakavyokuwa mgeni aliyeishi kati
yenu. Atafanya kama mnavyofanya mbele ya BWANA. 16 Sheria na amri hiyohiyo
ndiyo itakayotumika kwa mgeni anayeishi kati yenu." 17 Tena BWANA akanena
na Musa, akasema, 18 "Nena wana wa Israeli uwaambie, 'mtakapofika katika nchi
ninayowapeleka, 19 mtakapokula chakula kinachozalishwa katika nchi hiyo, mtatoa
sadaka ya kunipendeza mimi. 20 Kutoka kwenye mikate yenu ya kwanza mtatoa
mkate wa kuinuliwa kama sadaka iliyoinuliwa kutoka mahali pa kupuria nafaka.
Mtaiinua kwa jinsi hii. 21 Watu wa uzao wako wote wtanitolea sadaka ya kuinuliwa
kutoka kwenye unga wenu wa kwanza. 22 Wakati mwingine mtafanya dhambi pasipo
kukusudia, Kama hamtatii amri zote hizi ambazo nimemwambia Musa 23 -kila kitu
ambacho nimewaamuru kupitia Musa kuanzia siku ambayo nilianza kuwaamuru na
kuendelea kwa watu wote wa uzao wako. 24 Kwa swala la dhambi isiyokusudiwa
ambayo watu wote hawaijui, basi watu wote watatoa fahari mchanga sadaka ya
kuteketezwa ili kufanya harufu nzuri kwa BWANA. Pamoja na haya yote, lazima
itengenezwe sadaka ya unga na sadaka ya kinywaji, kama ilivyoagaizwa katika amri,
na beberu mmoja kuwa sadaka ya dhambi. 25 Kuhani atafanya sadaka upatanisho
kwa watu wote wa Israeli. Watasemehewa kwa sababu dhambi haikukusudiwa.
Wametoa sadaka yao, sadaka iliyotengenezwa kwa moto kwa ajili yangu. Wameleta
sadaka yao kwangu iliyotengenezwa kwa moto. Wameleta sadaka yao ya uovu mbele
yangu kwa ajili ya kosa lao. 26 Ndipo watu wote wa Israeli watasamehewa, pia wageni
wote wanaoishi kati yao, kwa sababu watu wote walitenda dhambi pasipo kukusudia.
27 Kama mtu atatenda dhambi bila kukusudia, atatoa mbuzi jike wa umri wa mwaka
mmoja kuwa sadaka ya dhambi. 28 Naye kuhani atafanya upatanisho kwa BWANA
kwa ajili ya mtu yule aliyefanya dhambi pasipo kukusudia. Yule mtu atasamehewa
baada ya upatanisho kufanyika. 29 Mtakuwa na sheria hiyohiyo kwa mtu yeyote
anayefanya dhambi hiyo pasipo kukusudia, sheria hiyohiyo hata kwa mzawa wa
Isreli na kwa wageni wanaoishi kati yao. 30 Lakini mtu afanyaye chochote kwa
KUkusudia, awe mzawa au mgeni, ananikufuru mimi. Huyo mtu ataondolewa kati ya
watu wake. 31 Kwa sababu atakuwa amedharau neno langu na amevunja neno amri
yangu, mtu huyo ataondolewa kabisa. Dhambi yake itakuwa juu yake.'" 32 Wakati
wana wa Israeli walipokuwa katika jangwa, wakamuona mwanamume akikusanya
kuni sikiu ya Sabato. 33 Wale waliomwona wakamleta kwa Musa, Haruni na kwa watu
wote. 34 Wakamweka kifungoni kwa sababu ilikuwa haijaamuliwa atakachotendewa.
35 Kisha BWANA akanena na Musa, "Yule mwanamume lazima auawe. Watu wote
lazima wampige kwa mawe nje ya kambi." 36 Kwa hiyo watu wote wakamtoa nje
ya kambi nao wakampiga kwa mawe mpaka akafa kama vile BWANA alivyokuwa
amemwamuru Musa. 37 BWANA akanena na Musa tena, akasema, 38 "Waambie
wana wa Israeli na uwaamuru wajifanyie vishada wavining'inize katika mapindo
ya mavazi yao, wavining'ineze katika ncha zote kwa nyuzi za rangi ya samawi. Watu
wote watafanya hivi kwa watu wote wa kizazi chote. 39 Huu utakuwa ukumbusho
maalumu kwenu, kila mtakapovitazama, mtakumbuka amri zangu, na kuzishika ili

kwamba msije mkatangatanga katika mioyo na macho yenu na kuwa waasherati
wa hayo. 40 Fanyeni hivi ili kwamba mweze kukumbuka na kutii amri zangu zote,
na ili kwamba mpate kuwa watakatifu, waliotunzwa kwa ajili yangu, Mungu wenu.
41 Mimi ndimi BWANA Mungu wenu niliyekutoa toka nchi ya Misri, ili niwe Mungu
wenu. Mimi ndimi BWANA Mungu wenu."

# 16

1 Sasa Kora mwana wa Izihari mwana wa Kohathi mwana wa Lawi, pamoja na
Dathani na Abiramu mwana wa Eliabu, na Oni mwana wa Peleti, wa uzao wa
Reubeni, waliwakusanya wanaume kadhaa. 2 Wakamwinukia Musa, pamoja na
wanaume fulani kutoka wana wa Israeli, viongozi wa watu wapatao mia mbili
na hamsini waliokuwa wakifahamika katika ile jamii. 3 Walikusanyika pamoja
kumpinga Musa na Haruni. Wakawaambia, "Ninyi sasa mnatumia mamlaka zaidi ya
uwezo wenu! Watu wote wamejitenga, kila mmoja wao, na BWANA yuko pamoja nao.
Kwa nini mnajiinua sana juu ya watu wengine wa BWANA?" 4 Musa alipoyasikia hayo,
akalala kifudifudi. 5 Akamwambia Kora na wote aliokuwa nao, "Asubuhi BWANA
atafanya ijulikane ni nani walio wake na nani aliyetengwa kwa ajili yake. Atamleta
huyo mtu karibu na yeye. Yule anayemchagua atamleta karibu naye. 6 Fanya hivi,
wewe Kora na kundi lako. 7 Kesho mchukue vyetezo na muweke moto na ubani ndani
yake mbele ya BWANA. Yule ambaye BWANA amemchagua, atamtenga kwa BWANA.
Sasa imetosha ninyi watu wa uzao wa Lawi," 8 Tena Musa akamwambia Kora, "Sasa
unisililize, ninyi watu wa uzao wa Lawi: 9 Je ni jambo dogo kwenu kwamba Mngu
wa mbinguni amewatenga ninyi kutoka watu wa Israeli, ili awalete ninyi karibu na
yeye, ili mfanye kazi katika masikani ya BWANA na kusimama mbele ya watu ili
muwatumikie? 10 Amewasogeza karibu, na ndugu zako, wa uzao wa Lawi pamoja
nanyi, na sasa mnataka na ukuhani pia! 11 Hiyo ndiyo sababu wewe na kundi lako
mmekusanyika pamoja kinyume na BWANA. Kwa nini mnalalamika juu ya Haruni,
ambaye anamtii BWANA?" 12 Kisha Musa akamwita Dathani na Abiramu, wana wa
Eliabu, lakini wakasema, "hatutakuja. 13 Kwani jambo dogo kwamba umetuleta
mpaka kwenye nchi inayotiririka maziwa na asali, ili kutuua katika jangwa hili?
Sasa unataka kujifanya kuwa mtawala wetu! 14 Na kwa nyongeza, haujatuingiza
kwenye nchi ya kutiririka maziwa na asali, au kutupa urithi wa mashamba na
mashamba ya mizabibu. Sasa unataka kutupofusha na ahadi hewa? Hatutakuja
kwako." 15 Musa alikasirika sana na akamwambia BWANA, "Usisipokee sadaka zao.
Sijachukua punda mmoja kutoka kwao, na sijamdhuru hata mmoja wao." 16 Kisha
Musa akamwambia Kora, "Kesho wewe na kundi lako mtaenda mbele za BWANA-
wewe na wao na Haruni. 17 Kila mmoja wenu atatwaa chetezo na kuweka ubani
ndani yake. Ndipo kila mtu atamletea BWANA chetezo chake, vyetezo mia mbili na
hamsini. Wewe na Haruni, pia, kila mmoja ataleta chetezo chake. 18 Kwa hiyo kila
mtu alitwaa chetezo chake, akaweka moto ndani yake, akaweka na ubani ndani yake,
na kusimama mbele ya lango la hema ya kukutania pamoja na Musa na Haruni.
19 Kora naye akawakusanya watu wote waliokuwa kinyume na Musa na Haruni
hapo kwenye lango la hema ya kukutania, na kisha utukufu wa BWANA ukaonekana
kwa watu wote. 20 Ndipo BWANA aliposema na Musa na Haruni: 21 "Tokeni ninyi
kutoka hawa watu ili nipate kuwaangamiza haraka." 22 Musa na Haruni wakalala
kifudifudi na kusema, "Mungu, Mungu wa wote wenye mwili, kama mtu akitenda
dhambi, ni lazima uwe na hasira na watu wote?" 23 BWANA akanena na Musa,
akamwambia, 24 "Sema na watu wote, uwaaambie, 'Tokeni kwenye hema ya Kora,
Dathani, na Abiramu.'" 25 Kisha Musa akaamuka akaenda kwa Dathani na Kwa
Abiramu; viongozi wa Israeli wakamfuata. 26 Akaongea na watu wote akasema,

“Sasa jitengeni na hema ya hawa watu waovu na msiguse kitu chochote kilicho
chao, vinginevyo mtaangamizwa na dhambi zao.” 27 Kwa hiyo watu wote toka
pande zote za hema ya Kora, Dathani na Abiramu wakaondoka. Dathani na Abiramu
wakatoka nje wakasimama kwenye lango la hema zao, wakiwa na wake wao, wana,
na watoto wao. 28 Kisha Musa akasema, “Kwa hili sasa mtatambua kuwa BWANA
amenituma kufanya kazi hizi zote, kwa kuwa sijazifanya kwa uwezo wangu. 29 Kama
hawa watu watakufa kifo cha kawaida ambacho humpata kila mmoja, basi BWANA
hakunituma. 30 Lakini kama BWANA aumbaye malango ya ardhi ambayo huwameza
kama mdomo mkubwa, pamoja na familia zao, na kama wataingia ndani ya shimo
wakiwa hai, ndipo mtakapojua kuwa wamemdharau BWANA,” 31 Mara ghafla Musa
alipomaliza kusema maneno haya, aridhi ya pale walipokuwa ikafunguka. 32 Dunia
ikafungua makanwa yake na kuwameza, familia zao na watu wote wa Kora, pamoja
na mali zao zote. 33 Wao na kila mmoja kwenye familia zao wakaingia ndani
shimoni wakiwa hai. Dunia ikwafunika, na kwa njia hii wakapotea kutoka miongoni
mwa ile jamii. 34 Nao Israeli yote waliokuwa karibu nao wakakimbia kwa sababu
ya vilio vyao. Walisema kwa mshangao, “Nchi isije kutumeza na sisi!” 35 Kisha
moto ukashuka toka kwa BWANA na kuwaangamiza wale wanaume 250 waliokuwa
wametoa ubani. 36 Tena BWANA akanena na Musa, akasema, 37 “Mwambie Eliazari
mwana wa Haruni yule kuhani achukue vile vyetezo kutoka ule moto, kwa kuwa
vile vyetezo vimetengwa ka ajili yangu. Na aumwage ule moto mbali. 38 Vitwae
vile vyetezo vya wale waliopoteza maisha yao kwa sababu ya dhambi zao. Na
vifanyike kuwa mbao za kufuliwa ili viwe vifuniko vya madhabahu. Kwa kuwa wale
watu walivitoa kwangu, kwa hiyo ni vitakatifu. Vitakuwa ishara ya uwepo wangu
kwa wana wa Israeli.” 39 Naye Eleazari yule kuhani akavichukue vile vyetezo vya
shaba ambavyo vilikuwa vimetumiwa na wale watu walioungua, na vikafuliwa kuwa
vifuniko vya madhbahu, 40 ili kuwa ukumbusho kwa wana wa Israeli, ili kwamba
asije akatokea mtu toka nje ya uzao wa Haruni akaja kutoa ubani kwa BWANA,
ili wasije kuwa kama Kora na kundi lake— kama vile BWANA alivyoamuru kupitia
kinywa cha Musa. 41 Lakini siku iliyofuata asubuhi watu wa Israeli wakamlalamikia
Musa na Haruni. Nao walisema, “Umeua watu wa BWANA.” 42 Kisha ikatokea,
wakati watu walipokuwa wamekusanyika kinyume na Musa na Haruni, wakatazama
kuielekea hema ya kukutania, na tazama lile wingu lilikuwa likiifunika. Utukufu
wa BWANA ukaonekana, 43 Musa na Haruni wakaja mbele ya hema ya kukutania.
44 Kisha BWANA akanena na Musa, akamwambia, 45 “Toka kati ya watu hawa
ili niwaangamize haraka.” Musa na Haruni wakalala chini kifudifudi. 46 Musa
akamwambia Haruni, uchukue chetezo, na utie ndani moto kutoka madhabahuni,
tia na uvumba ndani yake, upeleke haraka kwa watu, na ukafanye upatanisho kwao,
kwa sababu hasira hii inatoka kwa BWANA. Tauni imeanza.” 47 Kwa hiyo Haruni
akafanya kama alivyoelekezwa na Musa. Akakimbia kati ya watu. na Tauni ilikuwa
imeanza kuenea kati ya watu, kwa hiyo akaweka ndani yake uvumba na akafanya
upatanisho wa watu. 48 Haruni akasimama kati kati ya zile maiti na watu hai; na
kwa njia hii ile tauni ikazuiwa. 49 Idadi ya wale waliokuwa wamekufa kwa tauni
walikuwa14, 000, nje na wale waliokufa kutokana na swala la Kora. 50 Haruni akarudi
kwa Musa kwenye lango la hema ya kukutania, na ile tauni ikakoma.

# 17

1 BWANA akanena na Musa, akasema, 2 “Waambie wana wa Israeli wakuletee fimbo
za kutembelea moja kwa kila jamaa, fimbo kumi na mbili. Uandika jina la kila mmoja
kwenye hizo fimbo. 3 Utaandika jina la Haruni kwenye jina la Lawi. Kutakuwa na
fimbo moja kwa kila kiongozi kutoka kwenye kabila la mababu zake. 4 Utaziweka hizo

fimbo kwenye hema ya kukutania mbele ya amri za agano, ambapo Mimi hukutana
na wewe. Itakuwa hivi, [5] fimbo ya mtu yule ninayemchagua itachipua. Nitazuia watu
wa Israeli walalamikao, ambao wanaongea kinyume na wewe." [6] Kwa hiyo Musa
akawaambia wana wa Israeli. Viongozi wote wa kabila wakampatia fimbo, fimbo
moja kutoka kwa kila kiongozi, aliyechaguliwa kutoka kwenye kila kabila ya babu
zao, jumla yake fimbo kumi na mbili. Fimbo ya Haruni ilikuwa miongoni mwa fimbo
hizo. [7] Ndipo Musa alipoziweka zile fimbo mbele ya BWANA katika hema ya amri ya
agano. [8] Siku iliyofuata Musa aliingia kwenye hema ya amri ya agano, na tazama,
fimbo ya Haruni kwa ajili ya Kabila la Lawi ilikuwa imetoa machipukizi. Machipukizi
yalikuwa hadi kuchanua maua na kuzaa malozi mabivu! [9] Musa akazitoa fimbo zote
kutoka kwa BWANA kwa watu wote wa Israeli, na kila mtu akachukua fimbo yake.
[10] BWANA akamwambua Musa, "Iweke fimbo ya Haruni mbele ya amri za agano.
Iweke iwe ishara ya hatia mbele ya watu waliopinga ili ukomeshe malalamiko dhidi
yangu, vinginevyo watakufa." [11] Musa akafanya kama BWANA alivyoagiza. [12] Wana
wa Israeli wakanena na Musa wakisema, "tutakufa hapa! Wote tutaangamia! [13] Kila
mmoja anayekuja hapa, anayekaribia masikani ya BWANA, atakufa. Je, ni lazima
wote tuangamie?"

# 18

[1] BWANA akamwambia Haruni, "Wewe, wana wako, na uzao wa baba yako
watawajibika kwa dhambi zote zilizotendwa mahali patakatifu. Lakini wewe na
wana wako pekee mtawajibika kwa uovu uliofanywa na yeyote mahali patakatifu.
[2] Na ndugu zako nao wa kabila ya Lawi, kabila la ukoo wako, utawaleta pamoja
na wewe ili kwamba waweze kuungana na wewe ili wakusaidie wakati wewe na
wanao mnapokuwa mnatumikia mbele ya hema ya amri ya agano. [3] Watakutumikia
wewe na hema yote. Hata hivyo, wasisogee karibu na chochote ndani ya mahali
patakatifu au kitu chochote kilichounganishwa na madhabahu, vinginevyo wewe na
wao mtakufa. [4] Wataungana na wewe na kuitunza hema ya kukutania, kwa kazi
zote zinazohusiana na hema. Mtu mgeni asikusogelee. [5] Wewe utaajibika kwa ajili
ya mahali patakatifu na kwa ajili ya madhabahu ili kwamba hasira yangu isiwajilie
watu wa Israeli tena. [6] Tazama, Mmi mwenyewe nimewachagua ndugu zako wa
kabila ya Walawi kutoka mioingoni mwa uzao wa Israeli. Wao ni zawadi kwako.
walitolewa kwangu ili waifanye kazi inayohusiana na hema ya kukutania. [7] Lakini ni
wewe pekee yako na wanao ndio mnaoruhusiwa kufanya kazi ya ukuhani kuhusiana
na kila kitu kilichounganishwa na madhabahu na kitu chochote ndani ya lile pazia.
Wewe mwenyewe lazima ukamilishe majukumu hayo. Mimi ninakupa ukuhani
kama zawadi. Mgeni yeyote anayekaribia atauawa." [8] Kisha BWANA akamwambia
Haruni, "Tazama, Nimekupa majukumu ya kusimamia sadaka za kuinuliwa kwangu,
na sadaka zengine takatifu ambazo wana wa Israeli wanatoa kwangu. Nimekupa
sadaka hizi wewe na wana wako kuwa haki yako milele. [9] Hivi ni vitu vitakatifu
sana, amabavyo visiteketezwe kwa moto: kutoka kwenye sadaka zao-kila sadaka ya
unga, kila sadaka ya dhambi, na kila sadaka ya hatia- ni vitu vitakatifu sana kwa ajili
yako na wana wako. [10] Sadaka hizi ni takatifu sana; kila mume lazima aile, kwa kuwa
ni vitakatifu kwako. [11] Hizi ni sadaka ambazo zitakuwa zako: Sadaka zao, sadaka zote
za kuinuliwa za wana wa Israeli. Nimekupa wewe, wana wako na binti zako kuwa
gawio lako la milele. Kila mmoja ambaye ni msafi katika familia yako anaweza kula
sadaka zozote katika hizi. [12] Mafuta yote mazuri, ile divai nzuri yote mpya na unga,
malimbuko ambyo watu hutoa kwangu- vitu hivi vyote nimekupa wewe. [13] Mavuno
ya kwanza yaliyoiva yaliyo katika ardhi yao ambayo wanaleta kwangu, yatakuwa
yako. Kila mtu aliye msafi kwenye famila yako anaweza kula vitu hivi. [14] Kila

kitu kilichotolewa wakfu katika Israeli kitakuwa chako. [15] Kila kitu kinachofungua
tumbo, kila limbuko ambalo watu hutoa kwa BWANA, vyote vya watu na wanyama,
vitakuwa vyako. Hata hivyo, watu lazima wawakomboe wazaliwa wa kwanza wa
kiume, na watawakomboa wazaliwa wa kwanza wa wanyama wasio safi. [16] Wale
ambao wanahitaji kukombolewa na watu watakombolewa wakiwa na umri wa
mwezi mmoja. Ndipo watu watawakomboa kwa bei ya shekeli tano, kwa kiwango cha
shekeli za mahali patakatifu, ambacho ni sawa na gera ishirini. [17] Lakini mzaliwa wa
kwanza wa ng'ombe, au mzaliwa wa kwana wa kondoo, au mzaliwa wa kwanza wa
mbuzi-msiwakomboe hawa wanyama, wametengwa kwa ajili yangu. Utanyunyizia
damu yake madhabahuni na kuteketeza mafuta yao kama sadaka ya moto, ambayo
ni harufu nzuri ya kumpendeza BWANA. [18] Nyama yao itakuwa yako. Kama kidali
cha kuinuliwa na paja la kulia, nyama yao itakuwa yako. [19] Sadaka yote takatifu
ambayo watu wa Israeli wanaitoa kwa BWANA, nimekupa wewe, na wana wako na
binti zako walio pamoja nawe. Kama gawio la kudumu. Hili ni agano la milele la
chumvi, agano linalofunga milele, mbele za BWANA kwako wewe na uzao wako walio
pamoja na wewe." [20] BWANA akasema na Haruni. "hautakuwa na urithi katika ardhi
ya watu, wala hautakuwa na gawio miongoni mwa watu. Mimi ndimi gawiio lenu
na urithi wenu miongoni mwa watu wa Israeli. [21] Tazama, Nimewapatia uzao wa
Lawi, zaka zote za Israeli kuwa urithi wao kwa sababu ya huduma wanayotoa katika
hema ya kukutania. [22] Kuanzi a sasa, watu wa Israeli wasisogee karibu na hema
ya kukutania, vinginevyo wataajibika kwa dhambi hii na kufa. [23] Walawi wafanya
kazi inayohusiana na hema ya kukutania. Wataajibika kwa dhambi inyohusiana na
hema. Hii itakuwa sheri ya kudumu kwa watu wote wa uzao wako. Na miongoni
mwa watu wa Israeli hawa hawatakuwa na urithi. [24] Kwa kuwa zaka za wana wa
Israeli, wanazotoa kama mchango kwangu -ndivyo hivyo ambavyo nimewapa Walawi
kuwa urithi wao. Hiyo ndiyo sababu ya kuwaambia, Kuwa hawatakuwa na urithi
kati ya watu wa Israeli. [25] BWANA akanena na Musa, akamwambia, [26] "Inakupasa
ukaseme na Walawi uwaambie, 'Mnapopokea zaka toka kwa watu ambayo BWANA
amewapa kutoka kwao kuwa urithi, ndipo na nyie mtakapotoa sehemu ya kumi ya
zaka hizo. [27] Zaka yenu itahesabika kama moja ya mapato ya sakafu ya kupuria
nafaka ya mazao yenu au mazao ya vinu vya kukamulia zabibu. [28] Kwa hiyo na
ninyi lazima mtoe mchango wenu kwa BWANA kutokana na zaka mnazopata kutoka
kwa watu wa Israeli. Kutokana na hizo mtatoa matoleo yenu kwa Haruni yule
kuhani. [29] Kwa kila sadaka mnayopata, mtatoa matoleo yenu kwa BWANA. Mtafanya
hivi kutokana na vitu vizuri na vitakatifu sana ambavyo mmepewa. [30] Kwa hiyo
utawaambia, 'Mnapotoa hayo matoleo mazuri, ndipo itahesabika kwa Walawi kuwa
ni mazao yao kutoka kwenye sakafu za kupuria na vinu vyao vya kukamulia. [31] Ndipo
matakapokula nafaka zote zinazobaki mahali popote, ninyi na famailia zenu kwa
sababu ndiyo malipo yenu ya kazi y a kwenye hema ya kukutania. [32] Hamtakuwa
na hatia yeyote kwa kuvila na kuvinywa, kama mtatoa kwa BWANA matoleo yenu
mazuri mliyopokea. Lakini msizinajisi sadaka takatifu za wana wa Israeli, vinginevyo
mtakufa.,"

# 19

[1] BWANA akanena na Musa na Haruni, Akasema, [2] "Hii ni amri, ni sheria
ninayokuamuru: Waambie wana waIsraeli wakuletee ng'ombe mke mwekundu
asiyekuwa na kipaku wala waa, ambaye hajawahi kubeba nira. [3] Mpatie Eliazari
kuhani huyo ng'ombe jike. Naye atamtoa nje ya kambi, na mtu mmoja amchinje
mbele yake. [4] Kisha Eliazari kuhani atachukua sehemu ya damu yake kwa kidole
chake na kuinyunyiza mara saba akielekea sehemu ya mbele ya ile hema ya

kukutania. 5 Na kuhani mwingine atamchoma huyo ng'ombe mbele ya macho yake.
Ataichoma ngozi yake, nyama yake, na damu yake pamoja na mavi yake, 6 Yule
kuhani atachukua mti wa mwerezi, na hisopo na sufu na kivitupa katikati ya huyo
ng'ombe anayechomwa. 7 Kisha atazifua nguo zake na kuoga kwenye maji. Ndipo
atakuja kambini, ambapo atabaki najisi mpaka jioni ya siku hiyo. 8 Yule aliyemchoma
huyo ng'ombe mke atafua nguo zake kwa maji na kuoga majini. Naye atabaki najisi
mpaka jioni ya siku ile. 9 Baadaye mtu aliyesafi atayakusanya hayo majivu ya ng'ombe
huyo na kuyaweka nje ya kambi kwenye eneo safi. Majivu haya yatatunzwa kwa ajili
ya jamii ya watu wa Israeli. Watayachanganya majivu na maji kwa ajili ya utakaso wa
dhambi, kwa kuwa majivu yalitokana na sadaka ya dhambi. 10 Yule aliyeyakusanya
majivu ya ng'ombe huyo lazima afue mavazi yake. Atabaki najisi mpaka jioni ya siku
ile. Hii itakuwa sheria ya kudumu kwa watu wa Israeli na kwa wageni wanaoishi
nao. 11 Yeyote atakayegusa maiti ya mtu atakuwa najisi kwa siku saba. 12 Mtu wa
jinsi hiyo atajitakasa mwenyewe siku ya tatu na siku ya saba. Ndipo atakapokuwa
safi. Lakini kama hatajitakasa mwenyewe katika siku ya tatu, basi hatakuwa safi siku
ya saba. 13 Yeyote atakayegusa mtu aliyekufa, maiti ya mtu aliyekufa na hajajitakasa
- mtu huyu anainajisi masikani ya BWANA. Mtu huyo ataondolewa kuwa miongoni
mwa Waisraeli kwa sababu maji ya farakano hayakunyunyiziwa kwake. Atabaki
najisi; na unajisi wake utabaki kwake. 14 Hii ndiyo sheri ya mtu anayefia hemani.
Kila mtu aingiaye hemani na kila mtu ambaye tayari yumo hemani atakuwa najisi
kwa siku saba. 15 Kila chombo ambacho hakina kifuniko kinanajisika. 16 Vivyo hivyo,
kwa mtu aliye nje ya hema ambaye atamgusa mtu aliyeuawa kwa upanga, au mzoga
wowote, au mfupa wa mtu, au kaburi—mtu huyo atakuwa najisi kwa siku saba.
17 Fanyeni hivi kwa mtu najisi: twaeni majivu ya sadaka ya dhaambi ya kuteketezwa
na myacahanganye kwenye chombo chenye maji ya mto. 18 Ndipo mtu aliye safi
atachukua hisopo, na kutia katika hayo maji, na kunyunyizia juu ya hema, na katika
vyombo vyote vilivyo hemani, na kwa watu waliokuwepo, na kwa yule aliyegusa ule
mfupa, mtu aliyeuawa, maiti, au kaburi. 19 Katika siku ya tatu na siku ya saba, yule
mtu aliye msafi atamnyunyizia yule mtu asiyekuwa safi. Katika siku ya saba mtu
najisi atajitakasa mwenyewe. Atazifua nguo zake na kuoga kwenye maji. Jioni yake
atakuwa safi. 20 Lakini yule atakayebaki najisi, anayekataa kujitakasa mwenyewe
— huyo mtu ataondolewa kutoka kwenye jamii, kwa sababu amepanajisi patakatifu
pa BWANA. Hajanyunyiziwa maji ya utakaso; atabaki najisi. 21 Hii itakuwa sheria
ya kudumu kuhusiana na hali ya hivi. Yule mtu anayenyunyizia maji ya farakano
atafua mavazi yake. Yule atakayeyagusa maji ya farakano atakuwa najisi mpaka
jioni. 22 Chochote kile ambacho kitaguswa na mtu najisi kitakuwa najisi. na mtu
atakayekigusa naye atakuwa najisi mpaka jioni.

# 20

1 Kwa hiyo wana wa Israeli, na jamii yote ya watu, wakaenda katika jangwa la Sini
katika mwezi wa kwanza; wakaa Kadeshi. Hapo ndipo Miriamu alipofia na kuzikwa.
2 Huko hapakuwa na maji kwa ajili ya watu, kwa hiyo wakakusanyika kinyume na
Musa na Haruni huko. 3 Watu wakamlalamikia Musa. Wakasema, "Ilikuwa ni bora
kama tungelikufa wakati Waisraeli wenzetu walipokufa mbele za BWANA. 4 Kwa
nini umewaleta watu wa BWANA kufia katika jangwa hili, sisi na wanyama wetu?
5 Kwa nini ulitutoa Misri na kutuleta katika eneo hili baya? Hapa hakuna nafaka,
wala mitini, wala mizabibu, wala makomamanga. Na hakuna maji ya kunywa."
6 Basi Musa na Haruni wakatoweka mbele ya mkutano huo. Wakaenda kwenye
hema ya kukutania wakalala kifudifudi. Ndipo pale utukufu wa Busara wa BWANA
ukaonekana kwao. 7 BWANA akanena na Musa, akamwambia, 8 "Chukua fimbo yako

na uwakusanye watu, wewe na Haruni ndugu yako. Uumbie huu mwamba mbele ya
macho yao, na uumuru utoe maji. Nawe utawapa maji kutoka kwenye huu mwamba,
nawe utawapa maji ya kunywa hao watu na wanyama wao." 9 Musa akachukua
hiyo fimbo mbele ya BWANA, kama vile BWANA alivyokuwa amemwamuru kufanya.
10 Kisha Musa na Haruni wakawakusanya watu pamoja mbele ya ule mwamba. Ndipo
Musa akawaambia, "Sasa sikilizeni, enyi wapinzani. Lazima tuwape maji kutoka
kwenye huu mwamba?" 11 Ndipo Musa akanyosha mkono wake na kuupiga ule
mwamba mara mbili kwa fimbo yake, na maji mengi yakatoka. Wale watu wakanywa
pamoja na wanyama wao. 12 Kisha BWANA akamwambia Musa na Haruni, "Kwa
kuwa hamkuniheshimu mimi na kuniamini mbele ya watu wa Israeli, hamtawaingiza
hawa watu katika nchi niliyowaahidi. 13 Mahali hapa paliitwa maji ya Meriba kwa
sababu wana wa Israeli walitofautiana na BWANA pale, na akajionyesha kwao kuwa
mtakatifu. 14 Musa akatuma wajumbe kutoka Kadeshi kwa mfalme wa Edom: Ndugu
yako Israeli anasema hivi: "Wewe unajua magumu yote ambayo yametupata. 15 Na
unajua kuwa babu zetu walienda Misri na waliishi Misri kwa muda mrefu. Wamisri
walitutendea vibaya pamoja na babu zetu. 16 Tulipomlilia BWANA, akatusikia na
kututumia malaika ambaye alitutoa toka Misri. Tazama, sasa tuko Kadeshi, mji
unaopakana na nchi yako. 17 Tunakuomba uturuhusu kupita katika nchi yako.
Hatutapita mashambani wala kwenye mashamba ya mizabibu, wala hatutakunywa
maji ya visima vyako. Tutapita kwenye njia kuu ya mfalme. Hatutageuka upande wa
kulia wala upande wa kushoto mpaka tutakapopita mpaka wako." 18 Lakini mfalme
wa Edomu akamjibu, "Msipite hapa. Kama mtafanya hivyo, Nitakuja na upanga
kukuvamia." 19 Ndipo wana wa Israeli wakamwambia,"tutapitia njia kuu. Kama
sisi au wanyama wetu watakunywa maji yako, basi tutalipa. Tunaomba uturuhusu
tupite tukitembea kwa miguu yetu, bila kufanya jambo lolote lile." 20 Lakini mfalme
wa Edomu akajibu, "Usipite hapa." Kwa hiyo nfalme wa Edomu akawa kinyume
cha Israeli kwa mkono wenye nguvu pamoja na jeshi kubwa sana. 21 Mfame wa
Edomu akawazuia wana wa Israeli kupita kwenye mipaka yake. Kwa sababu ya
hili, Israeli akageuka kuiacha nchi ya Edomu. 22 Kwa hiyo watu wakasafiri kutoka
Kadeshi. Wana wa Israeli, watu wote, wakafika Mlima Hori. 23 BWANA akanena na
Musa na Haruni hapo kwenye Mlima Hori, kwenye mpaka wa Edomu. Akasema,
24 "Sasa ni wakati wa Haruni kukusanyika na watu wake, hataingia katika nchi ile
niliyowaahidi wana wa Israeli. Hii ni kwa sababu ninyi wawili hamkuitii sauti yangu
pale kwenye maji ya Meriba. 25 Mchukue Haruni na Eliazari mwanaye, na uwalete
juu ya Mlima Hori. 26 Umvulishi HarunI yale mavazi ya kikuhani na umvalishe
Eliazari mwanaye. Haruni atakufa na kulazwa pamoja na watu wake." 27 Musa
akafanya kama BWANA alivyomwamuru. Wakaenda juu y a Mlima Hori na watu
wote wakiona. 28 Musa akamvulisha Haruni yale mavazi ya kikuhani na kumvalisha
Mwanaye Eliazari. Haruni akafa pale juu ya Mlima Hori. Kisha Musa na Eliazari
wakashuka. 29 Watu walipoona kuwa Haruni amekufa, taifa lote wakamlilia Haruni
kwa siku arobaini.

## 21

1 Aradi mfalme wa Wakanaani, aliyekuwa akiishi Negebu, aliposikia kuwa Israeli
alikuwa akisafiri kwa kupitia barabara kuelekea Atharimu, akapigana dhidi ya
Israeli na kujitwalia baadhi ya mateka. 2 Israeli akaapa mbele ya BWANA
akasema, "Kama utatupa ushindi dhidi ya hawa watu, ndipo tutakapoingamiza
kabisa miji yao," 3 BWANA akaisikia sautiya Israeli na kuwapa ushindi dhidi ya
Wakanaani. Wakawaangamiza kabisa pamoja na miji yao. Mahali pale paliitwa
Horima. 4 Wakasafiri kutoka Mlima Hori kwa barabara kuelekea bahari ya shamu

wakiizunguka nchi ya Edomu. Watu walikufa moyo kwa njia hiyo. 5 Watu
wakamnung'unikia Mungu na Musa: “Kwa nini umetutoa Misiri ili tufa katika jangwa
hili? Hapa hakuna mikate, wala maji, na chakula hiki dhaifu kimetukinai.” 6 Basi
Mungu akatuma nyoka wa sumu kati yao. Wale nyoka wakawauma wale watu; watu
wengi walikufa. 7 Watu wakaenda kwa Musa wakamwambia, “Tumetenda dhambi
kwa sababu tumemnung'unikia Mungu na wewe. Mwombe Mungu atuondolee
hawa nyoka.” Kwa hiyo Musa akawaombea watu. 8 BWANA akamwambia Musa,
“Tengeneza nyoka na umweke kwenye nguzo. Na itakuwa kila anayeumwa,
akimwangalia huyo nyoka atapona,” 9 Kwa hiyo Musa akatengeneza nyoka wa shaba
naye akamweka juu ya nguzo. Na kila mtu alipoumwa na nyoka na kumwangalia
huyo nyoka alipona. 10 Kisha watu wa Israeli wakasafiri na kisha kuweka kambi
Obothi. 11 Kisha wakasafiri kutoka pale na kuweka kambi Iye Abarimu katika jangwa
linalokabili Moabu kuelekea upande wa mashariki. 12 Kutoka pale wakasafiri na
kuweka kambi katika bonde la Zeredi. 13 Kutoka pale walisafiri na kuweka kambi
kwenye upande mwingine wa mto Amoni, ambao ukubwa wake unaanzia kwenye
mpaka wa Waamori. Mto wa Amoni ndio unaootengeneza mpaka wa Moabu, kati
ya Moabu na Waamori. 14 Ndiyo maana imeandikwa katika gombo la Kitabu cha
BWANA, “Wahebu katika Sufa, na bonde la Amoni, 15 mtelemko wa bonde linaloelekea
katika mji wa Ari na kuelekea kwenye mpaka wa Moabu,” 16 Kutoka pale wakasafiri
mpaka Beeri, hapo ndipo palipo na kisima ambacho Bwana alimwambia Musa,
“Wakusanye watu kwa ajili yangu ili uwape maji,” 17 Ndipo Israeli waipoimba wimbo
huu: “enyi visima, yajazeni maji. Imbeni juu ya kisima hiki. 18 Kisima ambacho
viongozi wetu walichimba, kisima ambacho wenye hekima walichimba kwa fimbo
ya kifalme na kwa fimbo ya kutembelea.” Kisha kutoka jangwani walitembea mpaka
Matanaha. 19 Kutoka Matanaha walisafiri mpaka Nathalieli, na kutoka Nathalieli
mpaka Bamothi, 20 na kutoka Bamothi hadi kwenye bonde la Moabu. Hapo ndipo
kilele cha Mlima Piska kinapoonekana jangwani. 21 Kisha Israeli akatuma wajumbe
kwa Sihoni mfalme wa Waamori akisema, 22 Tunaomba tupite katika nchi yako.
hatutapita katika shamba au kwenye shamba la mizabibu. Hatutakunywa maji
ya visima vyako. Tutapita katika njia kuu ya mfalme mpaka tutakapopita mpaka
wako.” 23 Lakini mfalme Sihoni hakumruhusu Israeli kupita kwenye mpaka wao.
Badala yake, Sihoni akakusanya jeshi lake lote na kumvamia Isreli huko jangwani.
Akaja kwa Jahazi, ambapo alipigana dhidi ya Israeli. 24 Israeli akalivamia jeshi la
Sihoni na nchi ya upanga na kuchukua nchi yao kutoka Amon mpaka mto Jabboki,
hadi kufikia nchi ya watu wa Amoni. Sasa mpaka wa watu wa Amoni ulikuwa
umefungwa. 25 Israeli akachukua miji yote ya Waamori na akaishi ndani yake,
pamoja na Heshiboni na vijiji vyake wote. 26 Heshiboni ulikuwa mji wa Sihoni mfalme
wa Waamori, ambaye hapo awali alipigana dhidi ya mfalme wa kwanza wa Moabu.
Sihoni alikuwa ameteka ardhi yake yote toka mipaka yake mpaka mto wa Amoni.
27 Hiyo ndiyo sababu wala ambao huongea kwa Mitahali husema, “Njoni Heshboni.
Mji wa Sihoni ujengwe na kuimarishwa tena. 28 Moto uliwaka toka Heshiboni, moto
kutoka mji wa Sihoni ambao uliiteketeza Ari ya Moabu, na wenyeji wa miji ya juu
ya Amoni. 29 Ole wako, Moabu! umepotea, enyi watu wa Chemoshi. Amewafanya
watu wake kuwa wakimbizi na binti zake kuwa wafungwa wa Sihoni mfalme wa
Waamori. 30 Lakini tumempiga Sihoni. Tumeiangsmiza Heshibon mpaka Diboni.
Tumewaharibu wote mpaka Nofa, ambayo inafika mpaka Madeba.” 31 Kwa hiyo
Israeli akaanza kuishi katika nchi ya Waamori, 32 Kisha Musa akatuma watu kwenda
kuingalia Yaziri. Waliviteka vijiji vyake na kuwafukuza Waamori waliokuwa wakiishi
humo. 33 Kisha wakageuka na kuelekea njia inayoelekea Bashani. Ogu mfalme
wa Bashani akatofautiana nao, yeye na Jeshi lake lote, ili apigane nao kule Ederei.

[34] Kisha BWANA akasema na Musa, “Msimwogope, kwa sababu nimewapeni ushindi
dhidi yake, Jeshi lake lote na nchi yake. Mfanyeni kama mlivyomfanya Sihoni mfalme
wa Waamori, aliyekuwa akiishi Heshiboni.” [35] Kwa hiyo wakamuua, na wanawe, na
jeshi lake lote, mpaka wote wakaishi na hakubaki hata mmoja aliyebaki hai. Kisha
wakaichukua nchi yake.

# 22

[1] Watu wa Israeli wakasafiri mpaka wakaweka kambi kwenye uwanda wa Moabu
karibu na Yeriko, kwenye upande mwingine wa mto Yorodani kutoka mji ule.
[2] Balaki mwana wa Zippori aliona yote ambayo Israeli aliwafanyia Waamori. Moabu
aliogopa sana hao watu kwa sababu walikuwa wengi sana, [3] na Moabu alIwahofia
wana wa Israeli. [4] Mfalme wa Moabu akawaambia wazee wa Midiani, “Huu umati
utakula kila kitu tulicho nacho na maksai hula nyasi za kondeni.” Sasa Balaki
mwana wa Zippori alikuwa mfalme wa Moabu. [5] Akatuma wajumbe kwenda kwa
Balamu mwana wa Beori, kule Petho ambayo iko karibu na mto Frati, katika
nchi ya taifa lake na watu wake. Akamwita na kumwambia, “Tazama, Kuna
taifa ambalo wamekuja hapa tokea Misiri. Wanafunika uso wa dunia na sasa
wananifuatia mimi. [6] Tafadhali naomba uje unilaanie hili taifa, kwa sababu wana
nguvu kuliko mimi. Labda nitaweza kuwavamia na kuwafukuza watoke katika
nchi yangu. Najua kuwa yeyote unayembariki hubarikiwa na yeyote unayemlaani
atalaaniwa.” [7] Kwa hiyo wazee wa Moabu na wale wa Midiani wakaondoka,
pamoja nao wakachukua malipo ya uganga. Wakafika kwa Balaamu wakamwambia
maneno ya Balaki. [8] Balaamu akawaambia, “Bakini hapa usiku wa leo. Kesho
nitawaletea atakachoniambia BWANA.” Kwa hiyo wale viongozi wa Moabu wakabaki
na Balaamu kwa usiku huo. [9] Mungu akaja kwa Balaamu na kumwambia, “Ni akina
nani hawa waliokuja kwako?” [10] Balaamu akamjibu Mungu, “Balaki mwana wa
Zippori, Mfalme wa Moabu amewatuma kwangu. Alisema, [11] 'Tazama hawa watu
waliotoka Misri wanafunika uso wa nchi yangu. Sasa naomba uje unilaanie hawa
watu. Labada nitaweza kuwa kuwashinda na kuwafukuza.'” [12] Mungu akamjiu
Balaam, “Usiambatane na hao wanaume. Na usiwalaani hawa wana wa Israeli kwa
sababu wamebarikiwa.” [13] Balaamu akaamka asubuhi na kuwaambia wale viongozi
wa Balaki,. “Rudini nchini kwenu kwa sababu BWANA amenikataza kuambatana
nanyi.” [14] Kwa hiyo wale viongozi wa Moabu wakaondoka na kurudi kwa Balaki.
Wakamwambia, “Balaamu amekataa kuambatana nasi.” [15] Balaki akatuma viongozi
wengine waliokuwa wanaheshimiwa zaidi kuliko kundi lile la awali. [16] Wakaja kwa
Balaamu na kumwambia, “Balaki mwana wa Zippori anasema hivi, 'Tafadhali hebu
kitu chochote kisikuzuie kuja kwangu, [17] kwa sababu nitakulipa malipo mazuri sana
na kukupa heshima kubwa, nami nitakufanyia chochote utakachoniambia. Tafadhali
sana uje unilaanie hawa watu.'” [18] Balaamu akawajibu watu wa Balaki akawaambia,
“Hata kama Balaki atanipa ikulu yake ikiwa imejaa fedha na dhahabu, sitaweza
kufanya dhidi ya maneno ya BWANA, Mungu wangu na kufanya pungufu au zaidi
ya kile anachoniambia. [19] Sasa basi, tafadhali subirini hapa usiku wa leo pia, ili
kwamba nipate kujifunza kitu zaidi ambacho BWANA ananiambia.” [20] BWANA akaja
kwa Balaamu usiku ule na kumwambia, “kwa kuwa hawa watu wamekuja kukuita,
inuka uende nao. Lakini utafanya tu kile nitakachokuambia kufanya.” [21] Balaamu
akainuka asubuhi, akatandika punda wake, akaenda pamoja na viongozi wa Moabu.
[22] Lakini kwa sababu aliienda, hasira za Mungu zikawaka. Malaika wa BWANA
akasimama barabarani kama adui wa Balaamu, aliyekuwa akimpanda yule punda.
Watumishi wawili wa Balaamu walikuwa pamoja naye. [23] Yule punda alimwona
yule malaika wa BWANA akiwa amesimama barabarani akiwa na upanga mkononi

mwake. Yule punda akageuka na kwenda shambani. Balaamu akampiga yule punda
ili arudi barabarani. 24 Sasa malaika wa BWANA akasimama kwenye njia nyembamba
katikati ya mashamba ya mizabibu, na kushoto kwake kulikuwa na ukuta. 25 Yule
punda akamwona yule malaika wa BWANA tena. Akasogea zaidi ukutani na kuubana
mguu wa Balaamu ukutani. Balaamu akampiga tena yule punda. 26 Yule malaika
wa BWANA akasogea mbele zaidi kwenye eneo jingine jembamba zaidi ambalo
haikuwezekana kugeuka upande mwingine. 27 Yule Punda akamwona tena yule
malaika wa BWANA, akalala chini ya Balaamu. Hasira za Balaamu zikawaka,
akampiga yule punda kwa fimbo yake. 28 Kisha BWANA akafungua kinywa cha punda
na akaongea. Akamwambia Balaamu, “Nimekukosea nini kiasi kwamba umenipiga
mara tatu?” 29 Balaamu akamjibu yule punda, “Ni kwa sababu umenitendea kwa
ujinga. Natamani kama ningekuwa na upanga mkononi mwangu, kama ningekuwa
nao, sasa hivi ningekuwa nimekuua.” 30 Yule punda akamwambia Balaamu, “Je,
mimi si punda wako ambaye umenipanda maishani mwako mwote mpaka hivi
sasa? Je, nimewahi kuwa na tabia ya kukufanyia hivi hapo awali?” Balaamu
akasema “hapana.” 31 Basi BWANA akafungua macho ya Balaamu, na akamwona
malaika wa BWANA amesimama barabarani akiwa na upanga mkononi mwake.
Balaamu akainamisha kichwa chake chini. 32 Yule malaika wa BWANA akamwambia,
“Kwa nini umempiga punda wako mara tatu? Tazama, Nimekuja kama adui yako
kwa sababu matendo yako kwangu yamekuwa maovu. 33 Yule punda aliniona na
akageuka kutoka kwangu mara tatu. Kama asingekuwa amegeuka kutoka kwangu,
hakika ningekuwa nimekua na yeye kumwacha hai. 34 Balaamu akamwambia
malaika wa BWANA, nimetenda dhambi. Sikujua kuwa ulisimama kinyume na mimi
barabarani. Kwa hiyo sasa, kama haikupendezi, Nitageuka.” 35 Lakini yule malaika
wa BWANA akamwambia Balaamu, “endelea na wale watu. Lakini utasema maneno
nitakayokwambia tu.”Kwa hiyo Balaamu akaendelea na wale vioingozi wa Balaki.
36 Balaki aliposikia kuwa Balaamu alikuwa amekuja, alienda kukutana naye kule
mjini Moabu pale Amoni, ambao uko mpakani. 37 Balaki akamwambia Balaamu,
“Je, mimi sikutuma watu kukuita? Basi kwa nini hukuja kwangu? Je, mimi sina
uwezo wa kukufanya uheshimike?” 38 Ndipo Balaamu alipomjibu Balaki, “Tazama,
mimi nimekuja kwako. Je mimi sina mamlaka ya kusema chochote? Mimi ninaweza
kusema maneno ambayo Mungu ameweka kinywani mwangu.” 39 Balaamu akaenda
na Balaki, na Wakafika Kiriathi Huzothi. 40 Kisha Balaki akatoa sadaka ya maksai na
kondoo na kumpatia Balaamu baadhi ya hiyo nyama na wale viongozi waliokuwa
pamoja naye. 41 Kesho yake asubuhi, Balaki akampeleka Balaamu mpaka juu mahali
pa Baali. Kule juu Balaamu aliweza kuona sehemu tu ya kambi za Waisraeli.

# 23

1 Balaamu akamwabia Balaki, “Jenga madhabahu saba kwa ajili yangu na uandae
mafahari saba na kondoo dume saba.” 2 Kwa hiyo Balaki akafanya kama Balaamu
alivyoomba. Kisha Balaki na Balaamu wakatoa sadaka ya fahari mmoja na kondoo
dume mmoja kwa kila madhabahu. 3 Ndipo Balaamu alipomwamiba Balaki, “Simama
kwenye sadaka yako ya kuteketezwa na mimi nitaenda. Labda BWANA atakuja
kukutana na mimi. Chochote atakachoniambia nitakuambia.” Kwa hiyo akaenda juu
ya mlima usiokuwa na miti. 4 Wakati bado akiwa juu ya mlima. Mungu akakutana
naye, na Balaamu akamwambia, “Nimejenga madhabahu saba, na nimetoa sadaka
ya fahari na kondoo dume kwa kila madhabahu.” 5 BWANA akaweka ujumbe
kwenye kinywa cha Baalamu akasema, “Rudi kwa Balaki ukamwambie.” 6 Kwa
hiyo Balaamu akarudi kwa Balaki aliyekuwa amesimama karibu na sadaka yake ya
kuteketezwa, na viongozi wote wa Moabu walikuwa pamoja naye. 7 Ndipo Balaamu

alipoanza kunena unabii wake akisema, “Balaki amenileta kutoka Aramu, Mfalme
wa Moabu kutoka katika milima ya mashariki, 'Njoo, nilaanie Yakobo kwa ajili
yangu,' alisema, 'Njoo umtie unajisi Israeli,' 8 Nawezaje kuwalaani wale ambao Mungu
hajawalaani? Nawezaje kuwapinga wale ambao Mungu hawapingi? 9 Kwa kuwa
kutoka juu ya miamba Ninamwona; kutoka kwenye milima ninamtazama. Kuna
watu wanaoishi pekee yao na hawajioni wenyewe kama ni taifa la kawaida. 10 Nani
awezaye kuyahesabu mavumbi ya Yakobo au kuhesabu hata robo ya Israeli? Naomba
nife kifo cha mtu mwenye haki, na mwisho wa maisha yangu uwe kama wake!”
11 Balaki akamwambia Balaamu, “Umenifanyia nini? Nilikuleta ili uwalaani maadui
wangu, lakini ona, umewabariki,” 12 Balaamu akajibu akasema, “Kwa nini nisiwe
mwangalifu kusema kile ambacho BWANA anaweka kinywani mwangu?” 13 Basi
Balaki akamwambia, “Hebu uje nami kwenye eneo jingine ili uwaone. Utakaowaona
ni wale wa karibu tu, huwezi kuwaona wote. Huko sasa unaweza kunilaania hawa
watu.” 14 Kwa hiyo akampeleka Balaamu kwenye shamba la Zofimu, lililo juu ya
Mlima Pisiga, na kule akajenga madhabau zingine saba. Akatoa sadaka ya fahari
mmoja na kondoo dume kwa kila madhabahu. 15 Kisha Balaamu akamwambia Balaki,
“Simama hapa karibu na sadaka zako, wakati mimi naenda kukutana na BWANA
kule.” 16 Kwa hiyo BWANA akakutana na Balaamu na kumwekea ujumbe kinywani
mwake. Alimwambia, “Rudi kwa Balaki ukamwambie huu ujumbe toka kwangu.”
17 Balaamu akamrudia, na tazama, alikuwa amesimama karibu na sadaka zake za
kuteketezwa, na vionigozi wa Moabu walikuwa pamoja naye. Balaki akamwuliza,
“BWANA amekwambiaje?” 18 Balaamu akaanza kutoa unabii. Akasema, “Inuka,
Balaki na usikilize. Nisikilize mimi wewe mwana wa Zippori. 19 Mungu siyo mtu,
kwamba umdanganye, au mwanadamu awezaye kubadili mawazo. Je, alishawahi
kuahidi kitu pasipo kukitekeleza? Je, alishawahi kusema kuwa atafanya kitu bila
kufanya kama alivyosema? 20 Tazama, Mimi nimeamriwa kuwabariki. Mungu
ametoa baraka, nami siwezi kuibadilisha. 21 Hajawahi kuona magumu katika
Yakobo au tabu katika Israeli. BWANA Mungu wao yuko pamoja nao, na kelele
za wafalme wao ziko pamoja nao. 22 Mungu aliwatoa Misri kwa nguvu kama
za nyati. 23 Hakuna uganga utakaofanikiwa dhidi ya Yakobo, na hakuna uchawi
utakaomwumiza Israeli. Badala yake, itasemwa juu ya Yakobo na Israeli, 'Tazama
kile ambacho Mungu amefanya!' 24 Tazama, watu wanainuka kama simba jike, kama
vile simba ainukavyo na kuvamia. Halali chini mpaka ale windo lake na kunywa
damu ya windo lake,” 25 Kisha Balaki akamwambia Balaamu, “Kamwe usiwalaani
wala kuwabariki.” 26 Lakini Balaamu akamjibu Balaki, “Sijakuambia kuwa nitasema
yote ambayo BWANA ananiambia kusema? 27 Balaki akamwambia Balaamu, “Njoo
sasa, Nami nitakupeleka mahali pengine. Labda kule itampendeza Mungu kunilaania
hawa hawa watu.” 28 Kwa hiyo Balaki akampeleka Balaamu juu ya Mlima Peori,
ambao unalitazama chini lile jangwa, 29 Balaamu akamwambia Balaki, “Nijengee
madhabahu saba hapa na uniandalie mafahari saba na kondoo duume saba. 30 “Kwa
hiyo Balaki akafanya kama alivyoambiwa; akatoa sadaka ya fahari na kondoo mume
kwenye kila madhabahu.

# 24

1 Balaamu alipooa kuwa ilimpendeza BWANA kubariki Israeli, hakwenda, kama
hapo awali, kwa kutumia uganga, badala yake akatazama jangwani. 2 Akayainua
macho yake na kumwona Isreli akiwa kwenye kambi, kila mmoja kwa kabila yake,
na Roho wa Mungu akamjia. 3 Akapokea huu unabii na kusema, “Balaamu mwana wa
Beori anataka kusema, yeye ambaye macho yake yemefunuliwa sana. 4 Huongea na
kusikia maneno ya Mungu. Huona maono toka kwa Mwenyezi, ambaye mbele zake

humwinamia na macho yake yakiwa yamefumbuliwa. 5 Jinsi zilivyo nzuri hema
zako, ewe Yakobo, mahali unapoishi, Israeli! 6 Wamesambaa kama bonde, kama
bustani zilizo pembezoni mwa mto, Kama miti ya mishubiri iliyopandwa na BWANA,
ni kama mfano wa mielezi pembezoni mwa maji. 7 Maji yanatiririka katika ndoo
zao, na mbegu zao zimemwagiwa maji vizuri. Mfalme wao atakuwa juu ya Agagi,
na ufalme wao utaheshimiwa. 8 Mungu anamtoa Misri, na nguvu kama za nyati.
Atawameza mataifa wanaopigana nao. Ataivunja mifupa yao katika vipande vipande.
atawapiga kwa mishale yake. 9 Ananyatia kama simba mume, na kamaa simba jike.
Ni nani atakayejaribu kumsumbua? Kila mmoja anayembariki na abarikiwe; na kila
mmoja anayemlaani na alaaniwe." 10 Hasira za Balaki zikawaka dhidi ya Balaamu
naye akaipiga mikono yake kwa pamoja. Balaki akamwambia Balaamu, "Nilkuita
ili uwalaani maadui zangu, Lakini tazama, umewabariki mara tatu. 11 Kwa hiyo
ondoka uende nyumbani uniache sasa hivi. Nilisema ningekupa zawadi kubwa sana,
lakini BWANA amekuzuilia kupata zawadi." 12 Ndipo Balaamu alipomjibu Balaki,
"Niliwaambia wale wajumbe ulionitumia, 13 'Hata kama Balaki atanipa ikulu yake
ikiwa imejaa fedha na dhahabu, sitafanya zaidi ya maneno ya BWANA kwa lolote
zuri au baya, au kwa chochote ambacho ningetaka kufanya. Ninaweza kusema
kile tu ambacho BWANA ananiambia kusema,' Je, sikuwaambia haya? 14 Kwa hiyo
sasa, tazama, nitarudi kwa watu wangu. Lakini kwanza nikuonye kile ambacho
hawa watu watawafanyia watu wako katika siku zijazo." 15 Balaamu alianza unabii
huu. Akisema, "Balaamu mwana wa Beori anasema, Mtu yule aliyefumbuliwa
macho yake. 16 Huu ni unabii wa mtu alisikiaye neno la Mungu, aliye na maarifa
toka kwake Yeye aliye juu, aliye na maono kutoka kwa Mwenyezi, Yeye ambaye
humpigia magoti macho yakiwa yamefumbuliwa. 17 Ninamwona, lakini hayuko
hapa sasa. Ninamtazama, lakini siyo karibu. Nyota itatokea katika Yakobo, na
fimbp ya enzi itatokea katika Israeli. Naye atawapigapiga viongozi wa Moabu na
kuwaharibu wa uzao wa Sethi 18 Ndipo Edomu atakapokuwa miliki ya Israeli, na
Seiri pia itakuwa milki yao, maadui wa Israeli, ambao Israeli atawashinda kwa
nguvu zake. 19 Kutoka kwa Yakobo atatoka mfalme ambaye utawala wake naye
atawaangamiza waliosalia katika mji." 20 Kisha Balaamu akamtazama Amaleki
na akaanza kutoa unabii wake. Alisema, "Amaleki alikuwa mkuu katika mataifa,
lakini mwisho wake utakuwa uharibifu." 21 Kisha Balaamu akawatazama Wakeni
na akaanza kutoa unabii wake. Akasema, "Mahali unapoishi pana usalama, na
viiota vyake viko kwenye miamba. 22 Lakini pamoja na hayo, Kaini ataharibiwa
na Ashuru atakapowachukua mateka." 23 Kisha Balaamu akanza unabii wake wa
mwisho. Akasema, "Ole wake atakayesalia Mungu atakapoyafanya haya? 24 Merikebu
zitakuja toka pwani ya Kittimu; Zitaivamia Ashuru na kuiharibu Eberi, lakini wao
pia wataishia kwenye uharibifu." 25 Kisha Balaamu akainuka na kuondoka. Akarudi
nyumbani kwake, na Balaki naye akaondoka.

# 25

1 Israeli akakaa Shitimu, na wanaume wakaanza kufanya ukahaba na wanawake
wa Moabu, 2 kwa kuwa Wamoabu waliwakaribishsa kutoa sadaka kwa miungu
yao. Kwa hiyo watu wakala na kuisujudia miungu ya Moabu. 3 Watu wa Israeli
wakaungana kumwabudu Baali wa Peori, na hasira ya BWANA ikawaka dhidi ya
Israeli. 4 BWANA akamwambia Musa, "Waue viongozi wote wa watu na uwanyonge
mbele yangu ili waonekane wakati wa mchana, ili kwamba hasira yangu kali iondoke
kwa Israeli." 5 Kwa hiyo Musa akawaambia viongozi wa Israeli, "Kila mmoja wenu
lazima awanyonge watu wake ambao wameshiriki kumwabudu Baali wa Peori."
6 Kisha mtu mmoja wa Israeli akaleta mwanamke mmoja aliyekuwa miongoni mwa

familia yake. Hili lilitokea mbele ya macho ya Musa na watu wa Israeli, wakati
walipokuwa wakilia mbele ya lango la hema ya kukutania. 7 Finehasi mwana wa
Eliazari, mwana wa Haruni kuhani, alipoona hivyo, akainuka kutoka jamii ya watu
akachukua mkuki mkononi mwake. 8 Akamfuata yule mwanaume Muisraeli hemani
na kuwachoma kwa mkuki wote wawili kwenye miili yao, wote yule Muisraeli na
yule mwanamke. Kwa hiyo ile tauni ambayo Mungu alikuwa ameituma kwa watu
wa Israeli ikakoma. 9 Idadi ya wale waliokufa kwa tauni walikuwa elfu ishirini
na nne. 10 BWANA akanena na Musa, akasema, 11 "Finehasi mwana wa Eliazari
mwana wa Haruni, kuhani amaigeuza hasira yangu isiwe kwa wana wa Israeli kwa
sababu alikuwa na wivu kati yao juu ya wivu wangu. Kwa hiyo sijawaangamiza
watu wa Israeli kwa hasira yangu. 12 Kwa hiyo waambie, 'BWANA anasema, "Tazama,
Ninampa Finehasi agano la amani. 13 Kwake na kwa wana wake baada yake, litakuwa
agano la kudumu la ukuhani kwa sababu alikuwa na wivu juu yangu, Mungu wake.
Amewapatanisha wana wa Israeli. 14 Sasa yule Muisraeli aliyeuwawa pamoja na Yule
mwanamke Mmidiani alikuwa Zimri mwana wa Salu, kiongozi wa familia ya uzao wa
Simeoni. 15 Jina la yule Mmidiani aliyeuwawa lilikuwa Cozibi binti wa Zuri, ambaye
alikuwa mkuu wa familia wa kabila huko Midiani. 16 Kwa hiyo BWANA akanena na
Musa na kusema, 17 "Watendee Wamidiani kama maadui na uwaangamize, kwa kuwa
waliwatendea kama maadui 18 kwa kuwadanganya. Waliwaongoza katika uovu kwa
swala la Peori na kwa swala la dada yao Cozibi, binti wa kiongozi wa Wamidiani,
ambaye aliuawa siku ile ya tauni kwa swala la Peori."

# 26

1 Ilitokea baada ya tauni ambayo BWANA alimwambia Musa na Eliazari mwana wa
Haruni kuhani, Alisema, 2 Wahesabu watu wote wa Israeli, kuanzia miaka ishirini na
zaidi, kwa jamaa ya familia zao wote ambao wanaweza kwenda kwenye vita kwa
ajili ya Israeli." 3 Kwa hiyo Musa na Eliazari kuhani wakawaambia katika uwanda
wa Moabu karibu na Yorodani kule Yeriko na kusema, 4 Wahesabuni watu, kuanzi
umri wa miaka ishirini na zaidi kama BWANA alivyomwamuru Musa na watu wa
Israeli walitoka katika nchi ya Misri." 5 Reubeni ndiye aliyekuwa wa kwanza, Kutoka
kwa mwana wake Hanoki ulitokea ukoo wa Wahanoki. Kutoka kwa Palu ulitokea
ukoo wa Wapalu. 6 Kutoka Hezroni. ulitokea ukoo wa Wahezroni. Kutoka kwa Kami
ulitokea ukoo wa Wakami. 7 Hizi ndizo zilikuwa koo za uzao wa Reubeni, ambzo
idadi yao ilikuwa wanaume 43, 730. 8 Eliabu alikuwa mwana wa Palu. 9 Wana
wa Eliabu walikuwa ni Nemueli, Dathani. na Abiramu. Hawa ni walewale Dathani
na Abiramu waliomfuata Kora waliompinga Musa na Haruni na kumpinga BWANA.
10 Pale ambapo dunia ilifungua kinywa na kuwameza pamoja na Kora wakati ambapo
wafuasi wa Kora walikufa. Wakati ule, moto uliteketeza wanaume 250, amboa
wlikuwa ishara ya onyo. 11 Lakini uzao wa Kora haukufa. 12 Ukoo wa uzao wa
Simeoni walikuwa hawa wafuatao: Kutoka kwa Nemueli, ukoo wa Wanemueli, kwa
Jamini, ukoo wa Wajamini, kwa Jakini, ukoo wa Wajakini, 13 kwa Zera, ukoo wa
Wazera, kwa Shauli, ukoo wa Washauli. 14 Hizi ndizo koo za uzao wa Simeoni, idadi
yao ilikuwa wanaume 22, 200. 15 Koo za uzao wa Gadi zilikuwa hizi: Kwa Zefoni, Ukoo
wa Wazefoni, kwa Hagi, ukoo wa Wahagi, kwa Shuni, ukoo wa Washuni, 16 kwa Ozini,
ukoo wa Waozini, kwa Eri, ukoo wa Waeri, 17 kwa Arodi, ukoo wa Waarodi, kwa Areli,
ukoo wa Waareli. 18 Hizi ndizo koo za uzao wa Gadi, idadi yao walikuwa wanaume
40, 500. 19 Wana wa Yuda walikwa Er na Onani, lakini hawa walifia katika nchi ya
Kanaani. 20 Koo zingine za uzao wa Yuda zilikuwa hizi: Kwa Shela, ukoo wa Washela,
kwa Perezi, ukoo wa Waperezi, na kwa Zera, ukoo wa Wazera. 21 Uzao wa Perezi
walikuwa hawa: Kwa Hezroni, ukoo wa Wahezroni, kwa Hamuli, ukoo wa Wahamuli.
22 Hizi ndizo zilizokuwa koo za Yuda, idadi yao ilikuwa wanaume 76, 500. 23 Koo

za uzao wa Isakari zilikuwa hizi: Kwa Tola, ukoo wa Watola, kwa Puva, ukoo wa
Wapuva, 24 kwa Jashubu, ukoo wa Wajashubu, kwa Shimroni, ukoo wa Washimroni.
25 Hizi ndizo zilikuwa koo za Isakari, Idadi yao ilikuwa wanaume 64, 300. 26 Koo za
uzao wa Zabuloni zilikuwa hizi: Kwa Seredi, ukoo wa Waseredi, kwa Eloni, ukoo wa
Waeloni, kwa Jahaleeli, ukoo wa Wajahaleeli. 27 Hizi ndizo zilikuwa koo za Zabuloni,
idadi y ao ilikuwa wanaume 60, 500. 28 Koo za uzao wa Ysufu zilikuwa Manase na
Efraimu. 29 Huu ndio uliokuwa uzao wa Manase: Kwa Machiri, ukoo wa Wamachiri
(Machiri ndiye aliyekuwa baba wa Giliedi), kwa Giliedi, ukoo wa Wagiliedi. 30 Wazo
wa Giliedi walikuwa hawa wfuatao: Kwa Lezeri, ukoo wa Walezeri, kwa Helweki,
ukoo wa Waheleki, kwa Asrieli, 31 ukoo wa Asrieli wa Waasrieli, kwa Shekemu, ukoo
wa Washekemu, 32 kwa Shemida, ukoo wa Washemida, kwa Hefa, ukoo wa Wahefa.
33 Zelofehadi mwana wa Hefa hakuwa na watoto wa kiume bali alikuwa na mabinti.
Majina ya binti zake yalikuwa Mahilahi, Noha, Hoglaha, Milika, na Tiriza. 34 Hizi
ndizo koo za Manase, idadi yao ilikuwa wanaume 52, 700. 35 Koo za wana wa uzao
wa Efraimu zilikuwa hizi zifuatazo: Kwa Shuthelaha, ukoo wa Washutheleha, kwa
Becheri, ukoo wa Wabecheri, kwa Tahana, ukoo wa Watahana. 36 Uzao wa Shuthelaha
walikuwa, kwa Erani, ukoo wa Waerani. 37 Hizi ndizo koo za uzao wa Efraimu, idadi
yao ilikuwa wanaume 32, 500. Huu ndio uzao wa Yusufu, uliohesabiwa toka kila
koo zao. 38 Koo za uzao wa Benjamini zilikuwa hizi zifuatazo: Kwa Bela ukoo wa
Wabela, kwa Ashibeli, ukoo wa Washibeli, kwa Ahiramu, ukoo wa Wahiramu, 39 kwa
Shefufamu, ukoo wa Washefumamu, kwa Hufamu, ukoo wa Wahufamu. 40 Wana wa
Bela walikuwa ni Ardi na Naamani. Kutoka kwa Ardi ulijitokeza ukoo wa Waardi, na
kutoka kwa Naamani ukajaitokeza ukoo wa Wanaamani. 41 Hizi ndizo koo za uzao wa
Benjamini. Idadai yao ilikuwa wanaume 45, 600. 42 Kooo za uzao wa Dani zilikuwa
hizi zifuatazo: Kwa Shuhamu, ukoo wa Washuhamu. Hizi ndizo koo za uzao wa
Dani. 43 Idadi ya koo zote za Washuhamu ilikuwa wanaume 64, 400. 44 Koo za uzao wa
Asheri zilikuwa zifuatazo: Kwa Imna, ukoo wa Waimna, kwa Ishvi, ukoo wa Waishivi,
kwa Beria, ukoo wa Waberia. 45 Uzao wa Beria walikuwa hawa: Kwa Heberi, ukoo
wa Waheberi, kwa Malikieli, ukoo wa Wamalikieli. 46 Jina la binti wa Asheri lilikuwa
Sera. 47 Hizi ndizo koo za uzao wa Asheri, idadi yao ilikuwa wanaume 53, 400.
48 Koo za uzao wa Naftali zilikuwa zifuatazo: Kwa Jahazeeli, ukoo wa Wajahazeel,
kwa Guni, ukoo wa Waguni, 49 kwa Jezeri, ukoo wa Wajezeri, kwa Shilemu, ukoo
wa Washilemu. 50 Hizi ndizo zilizokuwa koo za uzao wa Naftali, idadi yao walikuwa
wanaume 45, 000. 51 Hii ndiyo iliyokuwa jumla kuu ya wanaume wa Israeli: 601, 730.
52 BWANA akanena na Musa akamwambia, 53 Ile ardhi itagawanywa kati ya wanaume
hawa kama urithi wao kwa kufuata idadi ya majina yao. 54 Kwa zile koo kubwa
utawagawia urithi mkubwa, na kwa koo ndogo ndogo utawagawia urithi kidogo. Kwa
kila familia utawapa urithi kufuata idadi ya wanaume waliohesabiwa. 55 Lakini ardhi
itagawiwa kwa kupigiwa kura. Watairithi nchi kama itakavyogawiwa kwa kufuata
koo za mababu. 56 Urithi huu utagiwiwa kufuata koo kubwa na ndogo, watagawiwa
kwa kufuata kura zitakavyokuwa. 57 Koo za Walawi, zilizohesabiwa kwa kufuata
ukoo kwa ukoo, walikuwa hivi: Kwa Gerishoni, ukoo wa Wagerishoni, kwa Kohathi,
ukoo wa Wakohathi, kwa Merari, ukoo wa Wamerari. 58 Koo za walawi zilikuwa hzi:
ukoo wa Walibni, Ukoo wa Wahebroni, ukoo wa Wamahali, ukoo wa Wamushi, na
ukoo wa Wakora. Kohathi alikuwa wa uzao wa Amramu. 59 Jina la mke wa Amramu
lilikuwa Jokibed, wa ukoo wa Lawi, aliyekuwa amezaliwa kwa Walawi kule Misri.
Alimzalia Amramu watoto wao, ambao walikuwa ni Haruni, Musa, na Miriamu dada
yao. 60 Kwa Haruni alizaliwa Nadabu na Abihu, Eliazari na Ithamari. 61 Nadabu
na Abihu walikufa walipotoa sadaka kwa BWANA sadaka ya moto isiyokubalika.
62 Waume walioheabaiwa miionigoni mwao walikuwa elfu ishirini na tatu, hawa nia
wale wa umri wa mwezi mmoja na zaidi. Lakini hawakuhesabiwa kati ya wazawa

wa Israeli kwa sababu hawakupewa urithi miongoni mwa wana wa Israeli. [63] Hawa
nadio wale walihesabiwa na Musa na Eliazari kuhani. Waliwahesabu watu wa Israeli
katika uwanda wa Moabu karibu na Yorodani kule Yeriko. [64] Lakini miongoni mwa
hawa hapakuwa na mwanamume aliyehasabiwa na Musa na Haruni kuhani wakati
wana wa uzao wa Israeli walipohesabiwa katika jangwa la Sinai. [65] Kwa BWANA
alikuwa amesema kuwa kwa hakika watu hao wote wangefia jangwani. Hapakuwa
na mtu aliyebaki miongoni mwao, isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune na Joshua
mwana wa Nuni.

# 27

[1] Kisah wakaja kwa Musa binti wa Zelofehadi mwana wa Hefa mwana wa
Gilied mwana wa Machiri mwana wa Manase, wa ukoo wa Manase mwana wa
Yusufu. Hawa ndio waliokuwa binti zake: Mahala, Noha, Hogla, Milika, na Tiriza.
[2] Walisimama mbele ya Musa, Eliazari kuhani, kwa. viongozi, na mbele ya watu
wote langoni mwa hema ya kukutania. Walisema, [3] "Baba yetu alifia jangwani.
Hakuwa mmoja wa wale waliompinga BWANA katika lile kundi la Kora. Alikufa
kwa dhambi zake, na hakuwa na watoto wa kiume. [4] Kwa nini jina la baba yetu
liondolewe mioingoni mwa ukoo wa jamaa zake kwa sababu ya kukosa wana? Tupeni
ardhi miongoni mwa ndugu wa baba zetu." [5] Kwa hiyo Musa alileta shauri hilo
mbele za BWANA. [6] BWANA akanena na Musa akamwambia, " Binti wa [7] Zelofehadi
wanasema kitu sahihi. Lazima uwaptie ardhi kama urithi miongoni mwa ndugu wa
baba zao, na uhakikishe kuwa urithi wa baba zao wanapata. [8] Utawaambia wana
wa Israeli na kusema, 'Kama mtu anakufa na hana mtoto wa kiume, basi utaufanya
urithi wake wapewe binti zake. [9] Kama hana binti, basi urithi wake atapewa kaka
zake. [10] Kama hana kaka zake basi huo urithi watapewa ndugu wa baba yake.
[11] Kama baba yake hana ndugu, basi huo urithi atapewa ndugu yake wa karibu
katika ukoo, na utauchukua kuwa wake. Hii itakuwa sheria iliyoanzishwa kwa amri
kwa ajili ya watu wa Israeli kama BWANA akivyoniamuru." [12] BWANA alimwamia
Musa, "Nenda juu ya mlima Abaraimu na uitazama nchi ambyo nimewapa wana wa
Israeli. [13] Baada ya kuwa umeiona, pia lazima ufe, kama Haruni kaka yako. [14] Hii
itatokea kwa sababu ulipinga amri yangu katika jangwa la Sini. Pale ambapo maji
yalitoka kwenye mwamba, katika hasira yako ulishindwa kuniheshimu mimi kama
mtakatifu mbele ya macho ya watu wote." Haya ni yale maji ya Meriba ya Kadeshi
katika jangwa la Sini. [15] Ndipo Musa akamwambia BWANA akisema, [16] "Wewe,
BWANA, Mungu wa wote wenye mwili, uchague mtu awe juu ya watu, [17] mtu ambaye
atatoka na kuingia kuja kwao na kuwatoa kisha kuwarudisha, ili kwamba watu
wako wasije kuwa kama kondoo wasiokuwa na mchungaji." [18] BWANA akanena
na Musa, "Mchukue Joshua mwana wa Nuni, mtu ambaye Roho yangu hukaa, na
umwekee mikono yako juu yake. [19] Umweke mbele ya Eliazari kuhani na mbele ya
watu wote, na umwamuru kuwaongoza mbele ya macho yao. [20] Utaweka baadhi ya
mamlaka yako kwake, ili kwamba watu wote wa Isareli wamtii. [21] Ataenda mbele
ya Eliazari kuhani ili kutafuta mapenzi yangu kwake kwa ajili ya maamuzi ya kura.
Yeye ndiyo atakayetoa amri ili watu kutoka na kuingia, yeye pamoja na watu wa
Israeli, ambao ni watu wote." [22] Kwa hiyo Musa akafanya kama alivyoagizwa na
BWANA. Alimchukua Joshua na kumweka mbele ya Eliazari kuhani na mbele ya
jamii yote. [23] Akaweka mikono yake juuy ake na kumwamuru aongoze, kama BWANA
alivyokuwa amemwamuru kufanya.

# 28

[1] BWANA akanena na Musa akamwambia, [2] "Waamuru wana wa Isrseli uwaambie,
'Mtanitolea sadaka kwa wakati uliopangwa, chakula cha sadaka yangu kilichoten-

genezwa kwa moto ili kutoa harufu nzuri kwa ajili yangu. 3 Pia uwaambie, 'Hii
ni sadaka iliyotengenezwa kwa moto ambayo mtaitoa kwa BWANA- mwanakondoo
dume wa mwaka mmoja asiyekuwa na waa, wawili kila siku kuwa sadaka ya
kuteketezwa ya kila siku. 4 Mwanakodoo mmoja atatolewa sadaka asubuhi, na
mwingine atatolewa sadaka jioni. 5 Mtatoa sadaka ya sehemu ya kumi ya efa
ya unga mwembamba kuwa sadaka ya unga, uliochanganywa na robo ya hini ya
mafuta yaliyokamuliwa. 6 Hii ni sadaka ya ya kuteketezwa ya kila siku iliyoamriwa
mlima Sinai ili kutoa harufu nzuri, sadaka iliyotengenezwa kwa moto kwa ajili
ya BWANA. 7 Pamoja na robo ya hini ya sadaka ya kinywaji kwa mmoja wa hao
wanakondoo. Utaimimina mahali patakatifu hiyo sadaka ya kinywaji kwa BWANA.
8 Yule mwanakondoo mwingine utamtoa sadaka jioni pamoja na sadaka ya unga
kama kama yule wa asubuhi alivyotolewa. Pia utatoa tena sadaka ya kinywaji pamoja
naye, sadaka iliyotengenezwa kwa moto ili kutoa harufu nzuri kwa BWANA. 9 Katika
siku ya Sabato utatoa wanakondoo dume wawili, wa umri wa mwaka mmoja kila
mmoja wasiokuwa na dosari, na sehemu ya kumi mbili ya efa ya unga mwembamba
kwa sadaka ya unga, uliochanganywa na mafuta, pamoja na sadaka ya kinywaji.
10 Hii itakuwa sadaka ya kuteketezwa kwa kila siku ya Sabato, kama nyongeza
ya ile sadaka ya kila siku pamoja na ile sadaka ya kinywaji. 11 Kila mwanzo wa
mwezi, mtatoa sadaka za kuteketezwa kwa BWANA. Utatoa sadaka ya fahari wawili
wachanga, kondoo dume mmoja, na wanakondoo dume saba wa umri wa mwaka
mmoja wasiokuwa na dosari. 12 Pia mtatoa sehemu ya kumi tatu ya efa unga
mwembamba kuwa sadaka ya unga uliochanganywa na mafuta kwa kila fahari, na
sehemu za kumi mbili za unga mwembamba kuwa sadaka ya unga uliochanganywa
na mafuta kwa yule kondoo mume mmoja. 13 Pia mtatoa sehemu ya kumi ya efa
ya unga mwembamba uliochanganywa na mafuta kuwa sadaka ya unga kwa kila
mwanakondoo. Hii itakuwa sadaka ya kuteketezwa, ya kutoa harufu nzuri, sadaka
iliyotengenezwa kwa moto kwa ajilI ya BWANA. 14 Sadaka ya kinywaji ya watu
itakuwa nusu ya hini ya divai ya yule fahari, sehemu ya tatu ya hini ya kondoo
dume, na robo ya hini ya mwanakondoo. Hii ndiyo itakuwa sadaka ya kuteketezwa
ya kila mwezi kwa miezi yote ya mwaka. 15 Mtatoa beberu mmoja kuwa sadaka ya
dhambi kwa BWANA. Hii itakuwa nyongeza kwa ile sadaka ya kila siku pamoja na
ile sadaka ya viinywaji. 16 Katika siku kumi na nne, ya mwezi wa kwanza itakuwa
Pasaka ya BWANA. 17 Katika sku ya kumi na tano ya mwezi huu kutakuwa na sikukuu.
Mtakuka mikate isiyo na chachu kwa siku saba. 18 Katika siku ya kwanza kutakuwa
na kusanyiko takatifu la kumheshimu BWANA. Katika siku hiyo msifanye kazi zenu
za kila siku 19 Hata hivyo, mtatoa sadaka iliyotengenezwa kwa moto, sadaka ya
kuteketezwa kwa BWANA. Mtatoa sadaka ya fahari wawili, kondoo dume mmoja, na
kondoo dume saba wa umri wa mwaka mmoja wakamilifu. 20 Pamoja na yule fahari,
mtatoa sadaka sehemu za tatu efa za unga mwembamba uliochanganywa na mafuta,
pamoja na yule kondoo mume sehemu za pili za kumi. 21 Kwa kila wale wanakondoo
saba, mtatoa sehemu ya kumi ya efa ya unga mwembamba uliochanganywa na
mafuta, 22 na beberu mmoja kuwa sdaka ya dhambi ili kufanya upatanisho kwa ajili
yenu. 23 Mtotoa hivi vitu kama sadaka ya nyongeza katika ile sadaka ya kila siku
inayotakiwa kila asubuhi. 24 Kama ilivyofafanuliwa hapa, mtatoa sadaka hizi kila
siku, kwa zile siku saba za Pasaka, kile chakula cha sadaka kilichotengenezwa kwa
moto kuwa harufu nzuri kwa BWANA. Hiki kitatolewa kuwa sadaka ya nyongeza
ya ile sadaka ya kuteketezwa na pamoja na ile sadaka ya vinywaji. 25 Siku ya saba
mtakuwa na kusanyiko takatifu ili kumheshimu BWANA, na katika siku hiyo msifanye
zile kazi zenu zakila siku. 26 Pia katika siku ya malimbuko, mtakapokuwa mnatoa
sadaka ya unga mpya katika sikukuu zenu za Majuma, mtakuwa na kusanyiko

takatifu la kumheshimu BWANA, na katika siku hiyo msifanye kazi zenu za kila
siku. [27] Mtatoa sadaka ya kuteketezwa ili kutoa harufu nzuri kwa BWANA. Mtatoa
fahari wawili wachanga, kondoo mume mmoja, na wanakondoo saba waume wa
mwaka mmoja. [28] Pamoja na hiyo mtatoa sadaka ya unga: unga mwembamba
uliochanganywa na mafuta, sehemu tatu za kumi za efa za unga mwembamba
uliochanganywa na mafuta kwa kila fahari na sehemu kumi mbili za yule kondoo
mume. [29] Toeni sehemu ya kumi ya efa ya unga mwembamba uliochanganywa na
mafuta kwa kila wale wanakondoo saba, [30] na beberu mmoja ili kufanya upatanisho
kwa ajili yenu. [31] Mtakapotoa hao wanyama wasio na dosari, pamoja na sadaka zake
za vinywaji, hii itakuwa sadaka ya nyongeza katika zile sadaka za kila siku na pamoja
na zile sadaka za unga.'"

# 29

[1] Katika siku ya kwanza, ya mwezi wa saba, mtakuwa na kusanyiko takatifu la
kumwabudu BWANA. Katika siku hiyo hamtafanya kazi zenu za kila siku. Itakuwa
siku ya kupiga matarumbeta. [2] Mtatoa sadaka ya kuteketezwa ya kufanya harufu
nzuri kwa BWANA. Mtatoa sadaka ya fahari mchanga, kondoo dume mmoja na
wanakondoo dume saba wa mwaka mmoja, kila mmoja mkamilifu. [3] Pamoja na
hao mtatoa sadaka ya unga, unga mwembamba uliochanganywa na mafuta, sehemu
tatu za kumi za efa kwa ajili ya huyo fahari, sehemu mbili za kumi kwa ajili ya huyo
kondoo mume, [4] na sehemu ya kumi ya kila hao wanakondoo waume saba. [5] Na
mtatoa beberu mmoja kuwa sadaka ya dhambi ili kufanya upatanisho kwa ajili yenu.
[6] Toeni hizo sadaka katika mwezi wa saba kama nyongeza ya sadaka mtakazotoa kila
mwanzo wa kila mwezi: pamoja na sadaka maalumu za kuteketezwa na sadaka za
unga. Hizi zitakuwa nyongeza za sadaka za kuteketezwa za kila siku, na sadaka
zake za unga, na sadaka zake za vinywaji. Utakapokuwa ukiendelea na sadaka hizi,
utakuwa ukitii kile kilichoamriwa kutoa harufu nzuri, sadaka iliyotengenezwa kwa
moto kwa BWANA. [7] Siku ya kumi ya mwezi wa saba, mtakuwa na kusanyiko takatifu
la kumwabudu BWANA. Mtajinyeneyekeza na hamtafanya kazi. [8] Mtatoa sadaka ya
kuteketezwa ili kutoa harufu nzuri kwa BWANA. Mtatoa fahari mmoja mchanga ili
kutoa harufu nzuri, kondoo mmoja mume, na wanakondoo saba waume wa mwaka
mmoja. Wote wakamilifu. [9] Pamoja na sadaka hizo utatoa sadaka ya unga, unga
mwembamba uliochanganywa na mafuta, sehemu tatu za kumi za efa kwa ajili ya
fahari, sehemu mbili za kumi za kondoo dume mmoja, [10] na sehemu ya kumi ya efa
moja kwa kila mwanakondoo wale saba. [11] Mtatatoa beberu mmoja kuwa sadaka
ya upatanisho. Hii itakuwa sadaka ya nyongeza ya upatanisho, ya sadaka ya kila
siku ya kuteketezwa, pamoja na sadaka za unga, na sadaka zake za vinywaji. [12] Siku
ya kumi na tano ya mwezi wa saba, mtakuwa na kusanyiko takatifu lakumwabudu
BWANA. Siku hiyo hamtafanya kazi za kila siku, na mtazitunza hizo sikukuu kwa
muda wa siku saba kwa ajili ya BWANA. [13] Mtatoa sadaka ya kuteketezwa, sadaka
iliyotengenezwa kwa moto ilikutoa harufu nzuri kwa BWANA. Mtatoa mafahari
wachanga kumi na tatu, kondoo waume wawili, na wanakondoo waume kumi na
nne wa mwaka mmoja. Wote wakamilifu. [14] Pamoja na hao mtatoa sadaka ya unga,
unga mwembaba uliochanganywa na mafuta, sehemu tatu za kumi za efa kwa kila
fahari katika hao kumi na tatu, sehemu mbili za kumi kwa kila hao kondoo dume
wawili, [15] na sehemu ya kumi ya efa ya hao wanakondoo kumi na nne. [16] Mtatoa
beberu mmoja kuwa sadaka ya dhambi katika nyongeza ya sadaka ya kuteketezwa,
sadaka yake ya unga, pamoja na sadaka za vinywaji. [17] Siku ya pili ya kusanyiko,
mtatoa mafahari kumi na mbili, kondoo dume wawili na wanakondoo dume kumi
na mbili wa umri wa mwaka mmoja, wote wakamilifu. [18] Pamoja nao mtatoa sadaka

ya unga, na sadaka ya vinywaji kwa ajili ya wale mafahari, kondoo dume, na kwa
ajili ya wale wanakondoo, mkitoa sadaka nyingi kama ilvyoamriwa. 19 Mtatoa beberu
mmoja kuwa sadaka ya dhambi kuwa nyongeza ya sadaka za kila siku, sadaka yake
ya unga, na sadaka zake za vinywaji. 20 Siku ya tatu ya kusanyiko, mtatoa sadaka
mafahari kumi na moja, kondoo dume wawili, na wanakondoo dume kumi na nne
wa umri wa mwaka mmoja, wakamilifu. 21 Pamoja na hizo sadaka mtatoa sadaka
ya unga na sdaka ya vinywaji kwa wale mafahari, kwa wale kondoo dume, na
kwa wale wanakondoo, utoe sadaka nyingi kama ilivyoamriwa. 22 Mtatoa sadaka
beberu mmoja kuwa sadaka ya dhambi kama nyongeza ya zile sadaka za kila siku,
na sadaka zake za unga, na sadaka zake za vinywaji. 23 Siku ya nne ya kusanyiko,
mtatoa mafahari kumi, kondoo dume wawili, na wanakondoo dume kumi na nne
wa mwaka mmoja, wakamilifu. 24 Pamoja na sadaka hizo mtatoa sadaka za unga
na sdaka za vinywaji kwa wale mafahari, na kwa wale kondoo dume na kwa wale
wanakodoo, mtatoa sadaka nyingi kama ilivyoamriwa. 25 Mtatoa beberu mmoja kuwa
sadaka ya dhambi kuwa nyongeza ya sadaka za kuteketezwa za kila siku, sadaka
zake za unga, na sadaka zake za vinywaji 26 Siku ya tano ya kusanyiko, mtatoa
mafahari tisa, kondoo dume wawili, na wanakondoo dume kumi na nne wa mwaka
mmoja, wakamilifu. 27 Pamoja na sadaka hizo mtatoa sadaka za unga na sadaka ya
vinywaji kwa ajili ya wale mafahari, kondoo dume, na wale wanakondoo, mkitoa
sdaka nyingi kama ilivyoamriwa. 28 Mtatoa beberu mmoja kuwa sadaka ya dhambi
kama nyongeza ya sadaka za kuteketezwa za kila siku, na sadaka zake za unga, na
sadaka za vinywaji. 29 Siku ya sita ya kusanyiko, mtatoa mafahari wanane, kondoo
dume wawili, na wanakondoo kumi na nne wa mwaka mmoja, wakamilifu. 30 Pamoja
na sadaka hizo mtatoa sadaka za unga nasadaka za vinywaji kwa wale mafahari,
kondoo wa dume na wale wanakondoo, mkitoa sadaka nyingi kama ilivyoamriwa.
31 Mtatoa beberu kuwa sadaka ya dhambi kama nyongeza ya sadaka za kila siku za
kuteketezwa, sadaka zadaka zake za unga, na sadaka zake za vinywaji. 32 Siku ya saba
ya kusanyiko, mtatoa mafahari saba, kondoo dume saba, na wanakondoo dume kumi
na nne wa mwaka mmoja, wakamilifu. 33 Pamoja nao mtataengeneza sadaka ya unga
na sadaka ya vinywaji kwa ajili ya wale mafahari, na kondoo dume, na kwa wale
wanakondoo, mkitoa sadaka nyingi kama ilivyoamriwa. 34 Mtatoa beberu mmoja
kuwa sadaka ya dhambi kama nyongeza ya sadaka ya kuteketezwa ya kila siku, na
sadaka yake ya unga, na sadaka yake ya vinywaji. 35 Siku ya nane mtakuwa na
kusanyiko lingine makini. Hamtafanya kazi zenu za kila siku. 36 Mtafanya sadaka za
kuteketezwa, sadaka iliyotengenezwa kwa moto ili kutoa harufu nzuri kwa BWANA.
Mtatoa fahari mmoja, kondoo mmoja dume, na wanakondoo saba dume wa umri
wa mwaka mmoja, wakamilifu. 37 Mtatoa sadaka zake za unga na sadaka zake za
vinywaji kwa ajili ya yule fahari, kondoo dume, na kwa wale wanakondoo, mkifanya
sadaka nyingi kadri ilivyoamriwa. 38 Mtatoa beberu mmoja kuwa sadaka ya dhambi
kama nyongeza ya sadaka za kila siku, na sadaka zake za unga, na sadaka zake
za vinywaji. 39 Hivi ndivyo utakavyotoa sadaka kwa BWANA katika sikukuu zenu
za kila mwaka. Hivi vitakuwa nyongeza ya viapo vyenu na sadaka zenu za hiari.
Mtavitoa hivi kama sadaka zenu za kuteketezwa, sadaka za unga, sadaka za vinywaji,
na sadaka za amani." 40 Musa aliwaambia wana wa Israeli kila kitu ambacho BWANA
alikuwa amemwamuru kusema.

# 30

1 Musa aliwambia viongizi wote wa makabila ya watu wa Israeli. "Hiki ndicho
ambacho BWANA ameamuru. 2 Mtu yeyote atakayefanya nadhiri kwa BWANA, au
kuapa kwa kiapo ili kufunga nafsi yake kwa ahadi, asivunje neno lake. Atafanya

sawa na ahadi yake imtokayo kinywani mwake. [3] Na kama binti anaishi katika
nyumba ya baba yake kwa atafanya nadhiri kwa BWANA na kuifunga nafsi yake
kwa kiapo, [4] na kama baba yake atasikia hiyo nadhirina ahadi ambayo ametumia
kuifunga nafsi yake, naye asiseme kitu kumzuia, ndipo nadhiri zake zitakuwa na
nguvu. Kila ahadi ambayo ameitumia kuifunga nafsi yake itabaki kuwa na nguvu.
[5] Lakini kama baba yake atasikia nadhairi yake na ahadi zake, na kama hatasema
chochote kwake, ndipo nadhiri zake zote na ahadi alizofanya zitakapokuwa na nguvu.
[6] Hata hivyo, kama baba yake atasikia nadhri zake zote alizofanya na ahadi zake
makini ambazo ametumia kufunga nafsi yake, na kama atazitengua ndani ya siku
hiyo, ndipo hizo nadhiri hazitakuwa na nguvu. BWANA atamsamehe kwa kuwa
baba yake amemzuia. [7] Kama ataolewa angali katika hivyo viapo, au kama atafanya
ahadi za bila kufikiri ambazo atajifunga nazo, hivyo vifungo vitakuwa na nguvu.
[8] Lakini kama mume wake atamzuia siku hiyo hiyo ambayo atamskia akiapa, basi
atabatailisha hicho kiapo alichokifanya, maneno yake ya midomo yaka ya bila kufikiri
ambayo kwayo amefunga nafsi yake. BWANA atamfungua. [9] Lakini kwa mjane
au kwa mwanamke aliyetalikiwa, kila kitu amabacho atakisema kufunga nafsi yake
lazima kitabaki na nguvu kinyume na yeye. [10] Na kama mwanamke atafanya kiapo
katika nyumba ya mume wake au akijifunga mwenyewe kwa kufanaya kiapo, [11] na
mume wake akakisikia hicho kiapo na hakusema chochote kwake na hakumpinga,
basi viapo vyake vitasimama na vifungo alivyovifanaya vitabaki na nguvu. [12] Lakini
kama mume wake atamzuilia katika siku hiyo ambayo atavisikia, basi chochote
ambacho kitatoka katika kinywa chake kuhusu viapo vyake au ahadi zake havitabaki
kuwa na nguvu. Mume wake atkuwa amevibatilisha. BWANA atamfungua. [13] Kila
kiapo ambacho mwanamke anakifanya ambacho kinamfunga ili kujikana kianaweza
kuthibitika au kubatilishwa na mume wake. [14] Lakini kama hatasema chochote
kwake siku baada ya siku, basi atathibitisha nadhiri zake na ahadi zake zinazomfunga
ambazo amefanya. Atakuwa amezithibitisha kwa sababu hakusema chochote wakati
alipozisikia. [15] Na kama mume wake atajariibu kubatilisha kiapo cha mke wake
baada ya kuzisikia kwa muda mrefu, basi ataajibika kwa dhambi zake." [16] Hizi
ndizo amri ambazo Mungu alimwamuru Musa kuzitangaza - amri ambazo ziko kati
ya mume na mke wake na kati ya baba na binti yake wakati akiwa katika ujana wake
katika familia ya baba yake.

# 31

[1] BWANA alinena na Musa na kumwambia, [2] "Uwalipizie kisasi Wamidiani kwa
kile walichowafanya Waisraeli. Baada ya kufanya hivyo utakufa na kukusanyika
na watu wako." [3] Kwa hiyo Musa akawaambia watu. Akasema, "andaeni baadhi
ya majeshi yenu kwa ajili ya vita ili kwamba wakawapige Wamidiani na kubeba
kiapo cha BWANA. [4] Kwa kila kabila la Israeli watatuma askari elfu moja kwa
ajili ya vita." [5] Kwa hiyo kati ya wanaume maelfu elfu wa Israeli, wanaume elfu
moja walitolewa kwa ajili ya vita, jumla ya wanaume elfu kumi na mbili. [6] Kisha
Musa akawatuma kwenda vitani, elfu moja toka kila kabila pamoja na Finehasi
mwana wa Eliazari kuhanai, wakiwa na vitu kutoka mahali patakatifu wakiwa
na matarumbeta kwa ajili ya ishara za sauti. [7] Wakapigana na Midiani, kama
BWANA alivyokuwa amemwamuru Musa. Wakamwua kila mwanaume. [8] Wakawaua
wafalme wa Midiani pamoja na wengine waliowaua ni: Evi, Rekimu, Zuri, Huri, na
Reba, hawa walaikuwa ndio waflme watano wa Midiani. pia walimwua Balaamu
mwana wa Beori, kwa upanga. [9] Jeshi la Israeli likawachukua mateka wanawake wa
Midiani, watoto wao, mifugo yao yote, kondoo wao na bidhaa zao zote. walivichukua
hivi kama mateka. [10] Waliichoma moto miji yao yote walimoishi na kambi zao

zote. 11 Walichukua vitu vyote na wafungwa, watu na wanyama. 12 Wakawaleta
mateka, nyara, na wakakamata vitu wakavileta kwa Musa, na Eliazari kuhani,
na kwa jamii ya watu wa Israeli. Wakavileta hivi vitu kambini katika uwanda
wa Moabu, kule Yorodani karibu na Yeriko. 13 Musa, Eliazari kuhani, pamoja na
viongozi wa watu wakaenda kukutana nao nje ya kambi. 14 Lakini Musa alikuwa
na hasira dhidi ya viongozi wa jeshi, Wale majemedari wa maelfu na maakida wa
mamia, waliotoka kupigana. 15 Musa akawaambia, “Je, mmeawaacha wanawake
wote kuishi? 16 Tazama, wanawake hawa ndio waliosababisha watu wa Israeli, kwa
kupitia ushauri wa Balaamu, kufanya dhambi dhidi ya BWANA huko Peori, wakati ile
tauni iliposambaa kwa watu wa Mungu. 17 Sasa basi, ueni kila mwanaume kuanzia
wadogo, na ueni kila mwanamke aliyelala na mwanamume. 18 Lakini chukueni
wale mabinti wadogo ambao hawajalala na mwanamume. 19 Mtaweka kambi nje
na kambi za Israeli kwa muda wa siku saba. Ninyi wote ambao mmeua watu au
ambao mmegusa maiti yeyote mtajitakasa wenyewe katika siku ya tatu na katika
siku ya saba - ninyi na mateka wenu. 20 Na mtayatakasa mavazi yenu yote, na kila
kitu kilichotengenezwa kwa ngozi za wanyama, na manyoya ya mbuzi, na kila kitu
kilichotengenezwa kwa mbao.” 21 Eliazarai kuahani akawaambia wale wanajeshi
waliokuwa wameenda vitani, “Hii ni amri ya sheria ambayo BWANA alimpa Musa:
22 Zile dhahabu, fedha, vyuma, bati, risasi, 23 na kila kitu knaweza kuhhimili moto,
mtakiweka katka moto, navyo vitakuwa safi. Nakisha mtavitakasa vitu hivyo na
maji ya farakano. Na vitu vyote ambavyo haviwezi kupita katika moto, mtavitakasa
kwa maji hayo. 24 Na mtazifua nguao zenu katika siku ya saba, ndipo mtakapokuwa
safi. Baada ya hapo mnaweza kurudi kwenye kambi za Israeli.” 25 Kisha BWANA
akanena na Musa, akamwambia, 26 “Vihesabu vitu vyote vilivyochukuliwa nyara,
wote watu na wanyama. Wewe, Eliazari kuhani, na viongozi wa watu kufuata koo
27 watavigawa hivi vitu katika mkundi mawili. Mvigawe kwa wanajeshi walioenda
kupigana na kwa watu wote. 28 Kisha toza kodi ambayo itatolewa kwangu kutoka
kwa wanajeshi waliokuwa wameenda vitani. Hii kodi itakuwa moja kati ya mia
tano, katika watu, ng'ombe, punda, kondoo, au mbuzi. 29 Uichukue hii kodi kutoka
katika nusu yao na umpe Eliazari kuhani kwa ajili ya sadaka itakayotolewa kwangu.
30 Pia kutoka katika nusu ya watu wa Israeli, utachukua moja kati ya hamsini -
kutoka vitu, ng'ombe, punda, na mbuzi. Uvitoe hivi kwa Walawi wanaotumika
katika masikani yangu.” 31 Kwa hiyo Musa na Eliazari kuhani wakafanya kama
BWANA alivyokuwa amemwamuru Musa. 32 Sasa zile nyara zilizokuwa zimebaki
ambazo wanajeshi walikuwa wameteka zilikuwa kondoo 675, 000, 33 maksai elfu
sabini na mbili, 34 punda elfu sitini na moja, 35 na wanawake elfu thelathini na
mbili ambao walikuwa hawajalala na mwanamume yeyote. 36 Ile hesabu ya nusu
iliyokuwa imetunzwa kwa ajili ya wanajeshi ilikuwa kondoo 337, 000. Ile sehemu
ya 37 BWANA ya kondoo ilikuwa kondoo 675. 38 Maksai walikuwa elfu thelathini na
sita ambayo kodi ya BWANA ilikuwa sabini na mbili. 39 Punda walikuwa 30, 500
ambao sehemu ya BWANA ilikuwa sitini na moja. 40 Watu walikuwa wanawake elfu
kumi na sita ambao kodi ya BWANA ilikuwa thelathini na mbili. 41 Musa aliichukua
ile kodi ambayo ilitakiwa kuwekwa sadaka kwa BWANA. Akampatia Eliazari kuhani,
kama BWANA alivyomwamuru Musa. 42 Ile nusu ya watu wa Israeli ambayo Musa
alikuwa ameichukua toka kwa wanawjeshi waliokuwa wameenda vitani - 43 ile nusu
y a watu ilikuwa kondoo 337, 500, 44 maksai elfu thelathini na sita, 45 punda 30,
500, 46 na wanawake elfu kumi na sita. 47 Kutoka kwenye nusu ya watu wa Israeli,
Musa alichukua moja katika hamsini, wote watu na wanyama. Aliwapa Walawi
ambao huitumikia masikani ya BWANA, kama BWANA alivyokuwa amemwamuru
kufanya. 48 Kisha wale maakida wa jeshi, makamanda wa elfu na makapteni wa

mamia, wakaja kwa Musa. [49] Wakamwambia, “watumishi wako wamewahesabu
wanajeshi ambao wako chini yetu, hakuna hata mmoja wao aliyekosa. [50] Tumemletea
BWANA sadaka, ambayo kila mmoja amepata, vitu vya dhahabu, metali, timbi, pete za
mhuri, vipini na vikuku, ili kujifanyia upatanisho kwa BWANA.” [51] Musa na Eliazari
kuhani akapokea kutoka kwao dhahabu na vitu vyote vilivyotengenezwa kwa ufundi.
[52] Vitu vyote vya sadaka ya dhahabu ambavyo walimpa BWANA- sadaka toka kwa
makamanda wa maelfu na kutoka kwa makepteni wa mamia - vilikuwa na uzito wa
shekeli 16, 750. [53] Kila mwanajeshi alikuwa ameteka nyara ya kila mtu kwa ajili
yake. [54] Musa na Eliazari kuhani wakazichukuazile dhahabu toka kwa makamanda
wa maelfu na makepteni wa mamia. Wakavipeleka kwenye hema ya kukutania kama
ukumbusho wa watu wa Israeli kwa BWANA.

# 32

[1] Sasa wana wa uzao wa Reubeni na wa Gadi walikuwa na idadi kubwa ya
wanyama. Waliiona ardhi ya Jazeri na Gileadi, kuwa ni ardhi nzuri kwa mifugo.
[2] Kwa hiyo wana wa Gadi na wa Reubeni wakaja kumwambia Musa, na Eliazari
kuhani, na viongozi wa watu. Wakasema, [3] “Hii ndiyo orodha ya maeneo ambayo
tumeyatembelea: Diboni, Jazeri, Nimraha, Heshibonni, Ellealehi, Sebamu, Nebo, na
Beoni. [4] Haya ni maeneo ambayo BWANA aliyachukua mbele ya watu wa Israeli, na
maeneo mazuri kwa ajili ya mifugo. Sisi watumishi wako tuna mifugo mingi sana.
[5] Wakasema kuwa, “Kama tutapata kibali mbele ya macho yako, tunaomba ardhi hii
tupewe, sisi watumishi wako, kuwa urithi. Usituvushe ng'ambo ya Yorodani.” [6] Musa
akawajibu wale wana wa auzao wa Gadi na Reubeni, “Je, mngependa ndugu zenu
waende vitani wakati ninyi mkikaa hapa? [7] Kwa nini kuwafish moyo watu wa Israeli
wasivuke kwenda kwenye nchi ambayo BWANA amewapa? [8] Baba zenu walifanya
hivyo nilipowatuma kutoka Kadeshi Banea kwenda kuipeleleza ile nchi. [9] Walienda
mpaka kwenye bonde la Eskoli. Waliiona ile ardhi kisha wakawafisha moyo watu wa
Israeli kwa hiyo wakagoma kuingia kwenye nchi ambayo BWANA alikuwa amewapa.
[10] Siku hiyo hasira ya BWANA iliwaka. Akaapa akisema, [11] 'Kwa hakika hakuna mtu
aliyetoka Misri, kuanzia wa umri wa miaka ishirini na zaidi ambao wataiona nchi
ambao niliwaapia Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, kwa sababu hawakunifuata mimi
kwa ukamilifu, isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune Mkenizi, na Yoshua mwana
wa Nuni. [12] Ni Kalebu na Joshua tu ndio walionifuata kwa ukamilifu.' [13] Kwa
hiyo hasira za BWANA ziliwaka juu ya Israei. Akawafanya wazunguke zunguke
jangwani kwa miaka arobaini mpaka kile kizazi kilichofanya maovu mbele za macho
yake kilipoteketea. [14] Tazama, mmetokea katika nafasi za baba zenu, kama watu
wengine wenye dhambi zaidi, ili kuongeza hasira ya BWANA kwa Israeli. [15] Kama
hamtamfuata, ataiacha Israeli jangwani na mtakuwa mmewateketeza watu hawa
wote. [16] Kwa hiyo wakaja karibu na Musa wakamwambia, “Turuhusu tujenga hapa
uzio kwa ajili ya ng'ombe zetu na miji hapa kwa ajili ya familia zetu. [17] Hata hivyo, sisi
wenyewe tutajipanga kijeshi kwenda na jeshi la Israeli mpaka tumewaongoza kupata
maeneo yao. Lakini familia zetu zitakuwa kwenye miji ya maboma kwa ssbabu ya
watu wengine ambao bado wanaishi katika nchi hii. [18] Hatutarudi kwenye familia
zetu mpaka kila mmoja watu wa Israeli apate urithi wake. [19] Sisi hatutachukua urithi
wa ardhi pamoja nao kule ng'ambo ya Yorodani, kwa sababu urithi wetu uko hapa
upande wa mashariki mwa Yorodani.” [20] Kwa hiyo Musa akawajibu, “Kama mtafanya
mnachokisema, kama mtajipanga wenyewe mbele za BWANA kwenda vitani, [21] basi
kila mmoja wa wanajeshi wenu lazima avuke Yorodani mbele za BWANA, mpaka
atakapowafukuza maadui zake kutoka mbele zake [22] na nchi itawaliwe na Israeli
mbele zake. Kisha mtaweza kurudi. Hamtakuwa na hatia mbele za BWANA na mbele

ya Israeli. Hii nchi itakuwa miliki yenu mbele za BWANA. 23 Bali kama hamtafnya
hivyo, tazama, mtakuwa mmefanya dhambi mbele ya BWANA. Mwe na hakika kuwa
dhambi yenu itaonekana 24 wazi. Jengeni miji kwa ajili ya familia zenu na mazizi
kwa ajili ya kondoo zenu; kisha fanyeni kile mlichokisema." 25 Wale wana wa Gadi
na Reubeni wakamwambia Musa, wakisema, "Watumishi wako wtafanya kama vile
wewe, bwana wetu, unavyotuamuru. 26 Watoto wetu, wake zetu, makundi yetu,
na wanyama wetu wote watakaa huko kwenye miji ya Gileadi. 27 Hata hivyo, sisi
watumishi wako, tutavuka kwenda ng'ambo mbele za BWANA kupigana, kila mtu
ambaye yuko tayari kwa vita, kama vile wewe, bwana wetu, unavyosema." 28 Kwa
hiyo Musa akawapa maelekezo yayowahusu kwa Eliazari kuhani, kwa Joshua mwana
wa Nuni, na kwa viongozi wa koo kufuata jamaa zao katika makabila ya wana wa
Israeli. 29 Musa akawaambia, "Kama uzao wa Reubeni na Gadi watavuka ng'ambo
ya Yorodani pamoja nanyi, kila mwanamume anayetakiwa kuwa vitani mbele za
BWANA, na kama nchi mtaitawala mbele zenu, ndipo mtakapowapa eneo la Gileadi
kuwa miliki yao. 30 Lakini kama hawatavuka pamoja nanyi wakiwa na silaha zao,
basi mtawapa urithi wao katika nchi ya Kanaani." 31 Kwas hiyo wana wa uzao wa
Gadi na wa Reubeni wakamjibu wakisema, Kama vile BWANA alivyosema nasi, sisi
watumwa wako, hiki ndicho tutakachokifanya. 32 Tutavuka tukiwa na silaha zetu
mbele za BWANA kuingia katika nchi ya Kanaani, lakini urithi wetu utabaki utabaki
upande huu wa Yorodani." 33 Kwa hiyo uzao wa Gadi na Reubeni, na pia nusu
ya kabila la Manase mwana wa Yusufu, Musa akawapa ufalme wa Sihoni, mfalme
wa Waamori, na wa Ogi, mafalme wa Bashani, Aliwapa hiyo nchi, na kuwagawia
miji yake yote pamoja na mipaka yake, miji yote ya nchi inayowazunguka. 34 Wale
wa uzao wa Gadi wakaijenga Diboni, 35 Atarothi, Aroeri, Atrothi, Jazeri, Jogbehaha,
Bethi Nimraha, 36 na Bethi Harani kuwa miji iliyo na maboma na mazizi ya kondoo
wao. 37 Wale wa uzao wa Reubeni wakaijenga Heshiboni. Elealehi, Kiriathaimu,
38 Nebo, Baali Meoni - baadaye waliyabadili majina yao, na Sibimaha. 39 Wale wa uzao
wa Machiri mwana wa Manase walienda Gileadi na kuutwaa kutoka kwa Waamori
waliokuwa wakiishi humo. 40 Kisha Musa akaitoa Gileadi kwa Machiri mwana wa
Manase, na watu wake wakaishi humo. 41 Jairi mwana wa Manase alienda kuiteka
miji yake na kuiita Havothi Jairi. 42 Nobaha alienda kuitieka Kenathi na vijiji vyake,
na akauita kwa jina lake Nobaha.

# 33

1 Hizi ndizo safari za wana wa Israeli hapo walipotoka katika nchi ya Misri pamoja
na makundi yao ya kijeshi chini ya uongozi wa Musa na Haruni. 2 Musa aliandika
maeneo yote tangu walipoondoka mpaka walipofika, kama alivyoamuriwa na
BWANA. Hizi ndizo safari zao kama kutoka kwao kulivyokuwa kwa kila walipotoka.
3 Mwezi wa kwanza walisafiri kutoka Ramesi, waliondoka siku ya kumi na tano.
Asubuhi siku iliyofuata baada ya Pasaka, Wana wa Israeli waliondoka wazi wazi,
mbele ya machoya Wamisri wote. 4 Hii ilitokea wakati Wamisiri walipokuwa
wakizika wazaliwa wao wa kwanza, ambao BWANA alikuwa amewaua miongoni
mwao, kwa kuwa pia alikuwa ameiadhibu miungu yao. 5 Wana wa Israeli walisafiri
kutoka Ramesi na kuweka kambi 6 Sukothi. Walisafiri toka Sukothi na kuweka
kambi Ethamu, mwisho wa nyika. 7 Wakasafiri kutoka Ethamu wakarudi mpaka
Pi-Hahirothi, ambayo inaikabili Baali Zephoni, ambapo waliweka kambi kuikabili
Migidoli 8 Kisha wakasafiri toka mkabala wa Pi-Hairothi na kupita katikati ya
bahari kuelekea nyikani. Wakasafiri safari ya siku tatu katika nyika ya Ethamu na
kuweka kambi Mara. 9 Wakasafiri kutoka Mara kufika Elimu. Pale Elimu kulikuwa
na chemichemi kumi na mbili za maji na miti sabini ya mitende. hapo ndipo
walipoweka kambi. 10 Walisafiri kutoka Elimu na kuweka kambi karibu na Bahari

ya Shamu. [11] Walisafiri kutoka Bahari ya Shamu na kuweka kambi katika nyika
ya Sini. [12] Walisafiri kutoka nyika ya Sini na kuweka kambi Dofka. [13] Wakasafiri
kutoka Dofka na kuweka kambi Alushi. [14] Wakasafiri kutoka Alushi na kuweka
kambi Refidimu, ambapo watu walikosa maji ya kunywa. [15] Walisafiri kutoka
Refidimu na kuweka kambi kwenye nyika ya Sinai. [16] Walisafiri kutoka nyika ya
Sinai na kuweka kambi Kibrothi Hataava. [17] Walisafiri kutoka Kibrothi Hataava na
kuweka kambi Hazerothi. [18] Walisafiri kutoka Hazerothi na kuweka kambi Rithima.
[19] Walisafiri kutoka Rithima na kuweka kambi Rimoni Perezi. [20] Walisafiri kutoka
Rimoni Perezi na kuweka kambi Libna. [21] Walisafiri kutoka Libna na kuweka kambi
Risa. [22] Walisafiri kutoka Risa na kuweka kambi Kehelatha. [23] Walisafiri kutoka
Kehelatha na kuweka kambi kwenye Mlima Sheferi. [24] Walisafiri kutoka Mlima
Sheferi na kuweka kambi Harada. [25] Walisafiri kutoka Harada na kuweka kambi
Makelothi. [26] Walisafiri kutoka Makelothi na kuweka kambi Tahathi. [27] Walisafiri
kutoka Ttahalathi na kuweka kambi Tera. [28] Walisafiri kutokaTera na kuweka kambi
Mithika. [29] Walisafiri kutoka Mithika na kuweka kambi Hashimona. [30] Walisafiri
kutoka Hashimona na kuweka kambi Moserothi. [31] Walisafiri kutoka Moserothi
na kuweka kambi Bene Jaakani. [32] Walisafiri kutoka Bene Jaakani na kuweka
kambi Hori Hagidigadi. [33] Walisafiri kutoka Hori Hagidigadi na kuweka kambi
Jotibatha. [34] Walisafiri kutoka Jotibatha na kuweka kambi Abrona. [35] Walisafiri
kutoka Abrona na kuweka kambi Ezioni Geberi. [36] Walisafiri toka Ezioini Geberi
na kuweka kambi katika nyika ya Sini kule Kadeshi. [37] Walisafiri kutoka Kadeshi na
kuweka kambi Mlima Hori, Pembezoni mwa nchi ya Edomu. [38] Hapo ndipo Haruni
kuhani alipoenda kwenye Mlima Hori kwa amri ya BWANA na kufa kule mwaka
wa arobaini bada ya Wisraeli kutoka katika nchi ya Misri, katika siku ya kwanza ya
mwezi wa tano. [39] Haruni alikuwa na umri wa mika 123 alipokufa pale juu ya Mlima
Hori. [40] Wakanaani, mfalme wa Aradi, ambao waliishi kusini mwa nyika katika nchi
ya Kanaani, walisikia juu ya ujio wa wana wa Israeli. [41] Walisafiri kutika Mlima
Hori n a kuweka kambi Zalimona. [42] Walisafiri kutoka Zalimona na kuweka kambi
Punoni. [43] Walisafiri kutoka Punoni na kuweka kambi Obothi. [44] Walisafiri kutoka
Obothi na kuweka kambi Abarimu, katika mpaka wa Moabu. [45] Walisafiri kutoka
Abarimu na kuweka kambi Diboni Gadi. [46] Walisafiri kutoka Diboni Gadi na kuweka
kambi Alimoni Diblathaimu. [47] Walisafiri kutoka Alimoni Diblathaimu na kuweka
kambi kwenye milima ya Abarimu mkabala na Nebo. [48] Walisafiri kutoka mlima
wa Abarimuna kuweka kambi kwenye nyanda za Moabu karibu na Yorodani huko
Yeriko. [49] Waliweka kambi karibu na Yorodani, kutoka Bethi Jeshimothi mpaka Abeli
Shitimu katika nyanda za Moabu. [50] Hapo BWANA alinenana Musa katika nyanda
za Moabu karibu na Yorodani kule Yeriko akasema, [51] “Nena na wana wa Israeli
uwaambie. 'Mtakapovuka mto Yorodani kuingia Kanaani, [52] ndipo mtakapowafukuza
wenyeji wote mbele yenu. Mtaziharibu sanamu zote za kuchongwa. Mtaziharibu
sanamu zao za kusubu na kuharibu mahali pao pote palipoinuka. [53] Mtachukua hiyo
ardhi iwe mali yenu na muishi ndani yake, kwa sababu nimewapeni hiyo nchi iwe
mali yenu. [54] Mtairithi hiyo nchi kwa kupiga kura, kwa kufuata kila ukoo. Kwa zile
koo kubwa kubwa mtawapa sehemu kubwa ya ardhi, na kwa zile koo ndogo ndogo
mtawapa sehemu ndogo ya ardhi. Kura itakapoanguka kwenye kila ukoo, hiyo ardhi
itakuwa mali yake. Mtairithi ardhi kufuata ukoo wa kabilla la jamaa zenu. [55] Lakini
kama hamtawafukuza wenyeji wa nchi hiyo watoke mbele yenu, ndipo wale watu
mtakaowaruhusu wakae nanyi watakapokuwa kama sindano machoni mwenu na
miiba katika mbavu zenu. Watayafanya maisha yenu yawe magumu katika nchi
mnayoishi. [56] Ndipo itakapotokea kuwa kile ambacho Mimi ninakusudia kufanya
kwa wale watu, Nitawafanyia pia ninyi'”

# 34

[1] BWANA akanena na Musa akasema, [2] “Waamuru watu wa Israeli na uwaambie,

'Mtakapoingia katika nchi ya Kanaani, nchi ambayo itakuwa mali yenu, nchi ya
Kanaani na mipaka yake, mpaka wenu wa kusini utaendelea kutoka nyika ya Sini
hadi mpaka wa Edomu. 3 Mwisho wa mpaka wa kusini utakuwa mwisho wa bahari
ya chumvi kuelekea mashariki. 4 Mpaka wenu utageukia kusini kutoka mlima
kuelekea Akrabimu na kupitia nyika ya Sini. na kutokea huko utaelelkea kusini mwa
Kadeshi Barinea na kuelekea Hazari Adari mpaka Azimoni. 5 Kutoka huko, mpaka
utageuka kutoka Azimoni kuelekea kijito cha Misri na kukifuata mpaka baharini.
6 Mpaka wa Magharibi utakuwa pwani ya bahari kuu. Huu ndio utakuwa mpaka
wenuwa Magharibi. 7 Mpaka wenu wa kaskazini utaanzia kwenye bahari kuu hadi
Mlima Hori, 8 kisha kutoka Mlima Hori hadi Lebo Hamathi, kisha Zedadi. 9 Mpaka
utaendelea hadi Zifroni na kuishia Hazari Enani. Huu ndio utakuwa mpaka wenu wa
kaskazini. 10 Kisha mtaweka alama za mpaka wenu wa mashariki ambao utaanzia
Hazari Enani kuelekea kusini Shefamu. 11 Kisha mpaka wa kusini utaendelea kutoka
Shefamu hadi Ribla, upande wa masharikia mwa Aini. Mpaka utaedelea upande huo
wa mashariki hadi upande wa mashariki wa bahari ya Kinerethi. 12 Kisha mpaka
utaendelea kuelekea kusini hadi mto Yorodani na hadi bahari ya chumvi. Hii ndiyo
itakuwa nchi yenu, kwa kuifuata mipaka yake yote inayozunguka.'" 13 Kisha Musa
akawaamuru watu wa Israeli akasema, "Hii ndiyo nchi ambayo mtaipokes kwa kura,
ambayo BWANA ameamuru kuwapa wale makabila tisa na nusu. 14 Kabila ya uzao
wa Reubeni, kwa kufuata jinsi walivyopewa urithi kwa jamaa ya kabila yao, na
uzao wa kabila la Gadi, kwa kufuata jinsi walivyopewa urithi kwa jamaa ya kabila
yao, na nusu ya Manase wamepata ardhi yao. 15 Wale makabila mawili na nusu
wameshapata mgawo wao ng'ambo ya mto Yorodani upande wa mashariki, kuelekea
kule linakotokea jua." 16 BWANA akanena na Musa akasema, 17 "Haya ndiyo majinaya
watu watakaoigawa ardhi kwa ajili ya urithi wao: Eliazari kuhani na Joshua mwana
wa Nuni. 18 Mtachagua kiongozi mmoja toka kila kabila ili kuigawa ardhi kwa koo
zao. 19 Haya ndiyo majina ya wanaume: Kutoka kabila la Yuda, Kalebu mwana wa
Yefune. 20 Kutoka kwenye kabila la uzao wa Simeoni, Shemueli mwana wa Amihudi.
21 Kutoka kabila la Benjamini, Elidadi mwana wa Kisloni. 22 Kiongozi kutoka kabila
la uzao wa Dani, Buki mwana wa Jogili. 23 Kiongozi kutoka uzao wa Yusufu, kwenye
kabila la Manase, Hannieli mwana wa Efodi. 24 Kiongozi kutoka kwenye kabila la
uzao wa Efraimu, Kemueli mwana wa Shiftani. 25 Kiongozi kutoka kabila la uzao
wa Zabuloni, Elizafani mwana wa Parinaki. 26 Kiongozi kutoka kwenye kabila la
uzao wa Isakari, Palitieli mwana wa Azzani. 27 Kiongozi kutoka kabila la uzao wa
Asheri, Ahihudi mwana wa Shelomi. 28 Kiongozi kutoka kabila la uzao wa Naftali,
Pedaheli mwana wa Amihudi." 29 BWANA aliwaamuru wanaume hawa kuigawa nchi
ya Kanaani na kuwapa kila kabla sehemu yao.

## 35

1 BWANA akanena na Musa kwenye nyanda za Moabu karibu na Yorodani kule
Yeriko akasema, 2 "Waamuru watu wa Israeli kutoa sehemu ya urithi wa ardhi yao
kwa Walawi. Watawapa miji ya kuishi ndani yake na eneo la malisho kuzunguka miji
hiyo. 3 Walawi watakuwa na miji hiyo ya kuishi. Eneo la malisho litakuwa kwa ajili ya
ng'ombe zao, kondoo zao, na wanyama wao wote. 4 Hayo malisho yatakayozunguka
miji hiyo ambayo mtawapa Walawi yataanzia kwenye maboma kwa ukubwa wa
"mita 457" kila upande. 5 Utapima dhiraa elfu mbili kutoka nje ya mji kuelekea
mashariki, na dhiraa elfu mbili kuelekea kusini, na dhiraa elfu mbili kuelekea upande
wa magharibi, na dhiraa elfu mbilii kuelekea upandewa kaskazini. Haya yatakuwa
maeneo ya malisho yao. Miji itakuwa katikati. 6 Katika hiyo miji sita mtakayowapatia
Walawi itatumika kama miji ya ukimbizi. Mtatoa maeneo haya ili kama mtu ameua

mtu apate mahali pa kukimbilia. Pia mtatoa miji mingine arobaini na mbli. 7 Jumla
ya miji ambyo mtawapa Walawi itakuwa arobaini na nane. Mtawapa hiyo miji
pamoja na maeneo yao ya malisho. 8 Zile kabila kubwa za watu wa Israeli, kabila
ambalo lina ardhi zaidi, watatoa ardhi zaidi. Makabila madogo madogo watatoa
miji michache. Kila kabila lazima watoe kwa ajili ya Walawi kwa kufuata mgawo
waliopata." 9 Kisha BWANA akanena na Musa akamwambia, 10 "Sema na wana wa
Israeli na uwaambie, 'Mtakapovuka Yorodani kuingia Kanaani, 11 Kisha mchague
miji itakayotumika kama miji ya ukimbizi kwa, ajili yenu, mahali ambapo mtu
aliyeua mtu pasipo kukusudia anaweza kukimbilia. 12 Hii miji itakuwa kwenu miji ya
ukimbizi kwa mtu anayetaka kulipa kisasi. ili kwamba mtuhumiwa asije akauawa
bila kwanza kusikilizwa na jamii. 13 Mtachagua miji sita kuwa miji ya ukimbizi.
14 Mtatoa miji mitatu kule ng'ambo ya Yorodani na miji mitatu huko Kanaani. Itakuwa
miji ya ukimbizi. 15 Kwa ajili ya watu wa Israeli, wageni, kwa, yeyote anayeishi
kati yenu, hii miji sita itatumika kama miji ya ukimbizi kwa mtu yeyote atakayeua
mtu bila kukusudia anaweza kukimbila. 16 Lakini kama mtuhumiwa amempiga mtu
na chombo cha chuma, na huyo mtu akafa, basi kwa hakika yule mtuhumiwa ni
muuaji. Kwa hiyo anatakiwa kuuawa. 17 Kama yule mtuhumiwa amempiga mtu kwa
jiwe mkonono mwake ambalo linaweza kumwua mtu, na kama yule mtu atakufa,
basi hakika huyo mtuhumiwa ni mwuaji. Kwa hakika anatakiwa kuuawa. 18 Kama
mtuhumiwa amempiga mtu kwa silaha ya mti ambayo inaweza kuua mtu na kama
huyo mtu atakufa, basi kwa hakika huyo mtuhumiwa ni mwuaji. kwa hakika huyo
anataikwa kuuawa. 19 Mwenye kulipa kisasi cha damu ndiye atakayemwua mwuaji.
atkapokutana naye, anaweza kumwua. 20 Lakini kama yule mtuhumiwa atamshinda
mtu yeyote yule anayemchukia au kama atamtupia kitu, wakati akimvizia, kiasi
kwamba huyo mtu akafa, 21 au kama atampiga ngumi kwa chuki na mtu huyo
akafa, ndipo yule mtuhumiwa aliyempiga hakika atauawa. Yeye ni mwuaji. Yule
mlipa kisasi cha damu anaweza kumwua muuaji pale atakapokutana naye. 22 Lakini
kama mtuhumiwa atampiga mtu ghafla bila kuwa na chuki hapo awali, au kama
atamtupia kitu ambacho kitampiga mtu bila kumvizia 23 au kama atatupa jiwe
amabalo linaweza kumwua mtu bila kumwona, basi huyo mtu hakua adui yake,
hakukusudia kumwumiza huyo mtu. Basi hiki ndicho kitachofanywa kama mtu
huyo atakufa. 24 Kwa tatizo la jinsi hiyo, Watu wataamua kati ya mlipa kisasi
na mtuhumiwa kwa kufuata taratibu zifuatazo. 25 Watu watamwokoa mtuhumiwa
kutoka kwenye nguvu za mlipa kisasi cha damu. Watu watamrudisha mtuhumiwa
katika mji wa ukimbizi ambao hapo awali alikimbilia. Ataishi pale mpaka yule
kuhani anayetumikia atakapokufa, ambaye alipakwa mafuta matakatifu. 26 Lakini
kama yule mtuhumiwa muda fulani ataenda nje ya mipaka ya mji a ukimbizi ambao
alikimbilia, 27 na kama yule mlipa kisasi cha damu atamwona nje ya mipaka ya
mji wake wa ukimbizi, kama atamwua huyo mtuhumiwa, mlipa kisasi cha damu
hatakuwa na hatia ya mauaji hayo. 28 Hii ni kwa sababu yule mtuhumiwa alitakiwa
kubaki katika mji wake wa ukimbizi mpaka kuhani mkuu atakapokufa. Baada ya kifo
cha kuhani mkuu, yule mtuhumiwa atarejea kwenye nchi yake ambako kuna mali
yake. 29 Hizi amri zitakuwa maagizo kwenu kwa kizazi chote mahali kote mnakoishi.
30 Yeyote amwuaye mtu, mwuaji atauawa, kama neno la ushahidi litakavyotolewa.
Lakini ushahidi wa mtu mmoja unaweza usitoshe kusababisha mtu kuuawa. 31 Pia,
msipokee fidia kwa ajili ya uhai wa mwuaji ambaye ana hatia ya mauti. Kwa hakika
lazima auawe. 32 Na msipokee fidia ya mtu aliyekimbilia kwenye miji ya ukimbizi.
Msimruhusu kwa namna yeyote kurudi kwenye mali zake mpaka pale kuhani mkuu
atakapokufa. 33 Msiiharibu nchi mnayokaa kwa namna hii, kwa kuwa damu ya
mwuaji huharibu nchi. Hakuna sadaka ya upatanisho inayoweza kufanywa kwa

nchi pale damu inapomwagika juu yake, isipokuwa kwa damu ya mtu aliyeimwaga.
34 Kwa hiyo msiinajisi nchi mnayoishi kwa sababu Mimi ninaishi ndani yake. Mimi
BWANA huishi kati ya watu wa Israeli.”'

# 36

1 Kisha wale viongozi wa nyumba za mababa wa ukoo wa Gileadi mwana wa
Machiri (ambaye alikuwa mwana wa Manase), ambao walikuwa wa ukoo wa uzao
wa Yusufu, walikuja wakasema mbele za Musa na mbele za vionigozi wa familia
za mababa wa watu wa Israeli. 2 Wakasema, “BWANA alikuamuru, wewe bwana
wetu, kutupa mgawo wa ardhi kwa kura kwa wana wa Israeli. Uliamuriwa na
BWANA kutoa mgawo wa Zerofehadi kaka yetu kwa binti zake. 3 Lakini hawa binti
wameolewa na wanaume toka kabila zingine za wana wa Israeli, basi mgawo wao
wa ardhi utaondolewa kutoka kwenye mgawo wa mababa zao. Utaongezwa kwenye
mgawo wa makabila ambayo wao wanaungana nao. Kwa sababu hiyo, Utaondolewa
kwenye mgawo uliopangwa kwenye urithi wetu. 4 Kwa sababu hiyo, wakati wa
mwaka wa yubilee ya wana wa Israeli utakapofika, mgawo wao utaunganishwa
na kabila ile waliyoungana nao. Kwa sababu hii mgawo wao utaondolewa kwenye
mgawo wa mababa zetu.” 5 Basi Musa akawapa amri wana wa Israeli, kwa neno la
BWANA. Akasema, “Kile wanachosema watu wa kabila la Yusufu kiko sahihi. 6 Hiki
ndicho BWANA anaagiza kuhusu mabinti wa Zelofehadi. Anasema, 'Acha waolewa
na wale ambao wao wanaofikri ni vizuri zaidi, lakini lazima waolewe ndani ya kabila
ya baba yao.' 7 Hakuna mgawo wa watu utakaobadilika kutoka kabila moja kwenda
jingine. Kila mtu wa Israeli ataendelea na mgawo wa kabila ya baba y ake. 8 Kila
mwanamke wa watu wa Israeli aliye na mgao kwenye kabila lake lazima aolewe
na mtu wa ukoo unaotoka kwenye kabila la baba yake. Hii itafanyika hivyo ili kila
mtu wa wana wa Israeli aweze kuwa na urithi kutoka kwa mababa zake. 9 Hakuna
mgawo utakaobadilika kutoka kabila nyingine kwenda kabila nyingine. Kila mtu wa
kabila za watu wa Israeli atalinda urithi wake.” 10 Kwa hiyo wale binti wa Zelofehadi
walifanya kama vile BWANA alivyokuwa amemwamuru Musa. Mahila, Tiriza, Hogila,
Milika, na Noha, binti za 11 Zelofehadi, waliolewa na wana wa uzao wa Manase.
12 Waliolewa katika koo za uzao wa Manase mwana wa Yusufu. Kwa sababu hii,
urithi wao ulibaki kwenye kabila la ukoo ambalo baba yao alikuwa anatoka. 13 Hizi
ndizo amri na maagizo ambayo BWANAaliyatoa kupitia Musa kwa wana wa Israeli
katika nyanda za Moabu karibu na Yorodani huko Yeriko.

# Kumbukumbu la Torati

[1] Haya ni maneno ambayo Musa aliyasema kwa Israeli wote ng'ambo ya jangwa
la Yordani, katika tambarare ya mto wa Yordani juu ya Suph, katikati mwa Paran,
Topheli, Laban, Hazeroth, na Di Zahab. [2] Ni safari ya siku kumi na moja toka Horabu
kupitia njia ya mlima wa Seir kwenda Kadeshi Barnea. [3] Ilitokea kwenye mwaka
wa nne, mwezi wa kumi na moja, siku ya kwanza ya mwezi, Musa alizungumza
kwa watu wa Israeli, kuambia yote yale Yahwe aliyomwamuru kuhusu wao. [4] Hii
ilikuwa baada ya Yahwe kumvamia Sihoni mfalme wa Amoria, ambaye aliishi huko
Heshboni, na Ogi mfalme wa Bashani, ambaye aliishi huko Ashtarothi ya Edrei.
[5] Ng'ambo ya Yordani, katika nchi ya Moabu, Musa alianza kutangaza maelekezo
haya, akisema, [6] “Yahwe Mungu wetu alisema nasi huko Horebu, akisema, umeishi
vya kutosha katika milima ya nchi hii. [7] Geuka na uanze safari yako, na uende kwenye
nchi ya milima ya Amorites, na kwenye maeneo yote karibu na tambarare ya mto
Yordani, katika nchi ya milima, na nyanda za chini, huko Negev, na pwani - nchi ya
Wakanani na huko Lebanoni mbali ya mto mkuu wa Euphratesi. [8] Tazama, nimetenga
nchi kwa ajili yako, nenda ndani na umiliki nchi ambayo Yahwe aliapa kwa baba
zako, Ibrahimu, Isaka na Yakobo, kuwapa na uzao wao baada yao. [9] Nilisema
nawe kwa wakati huo, nikisema, siwezi nikakubeba peke yangu, [10] Yahwe Mungu
wako amekuzidisha, na tazama, leo umekuwa umati wa nyota angani. [11] Yahwe
aweza, Mungu wa baba zako, kukufanya wewe mara elfu moja zaidi ya ulivyo, na
kukubariki, kama alivyokuahidi! [12] Lakini inawezekanaje mimi peke yangu kubeba
shehena zako, mizigo yako, na migogoro yako? [13] Chukua wanaume wa hekima,
wanaume waelewa, na wanaume walio na sifa nzuri toka kila kabila, nitawafaya
kuwa vichwa juu yenu. [14] Mlinijibu na kusema, 'Jambo ulilolisema ni zuri kwetu
kufanya.' [15] Kwa hiyo nilichukua vichwa vya makabila yenu, wanaume wa hekima,
na wanaume wenye sifa nzuri, na nikawafanya kuwa vichwa juu yenu, jemedari
kwa elfu, jemedari kwa hamsini, jemedari kwa kumi, na maakida, kabila kwa kabila.
[16] Niliwaamuru waamuzi wenu kwa wakati huo, kusema, 'Zikiliza mabishano kati
ya ndugu zenu, na muhukumu ya haki kati ya ndugu na ndugu zake, na mgeni
aliye pamoja naye. [17] Hamtaonesha upendeleo kwa yeyote katika mgogoro, mtasikia
madogo na makubwa pia. Hamtaogopa uso wa mtu, kwa kuwa hukumu ni ya
Mungu. Migogoro iliyo migumu kwenu, mtaniletea mimi, na mimi nitaisikiliza.
[18] Niliwaamuru kwa wakati huo mambo yote mtakayofanya. [19] Tulisafiri toka
Horebu na kwenda kupitia jangwa lile kubwa lote na lenye kutisha lile mliloliona,
katika njia yetu kuelekea nchi ya milima huko Amorites, kama Yahwe Mungu wetu
alivyotuamuru sisi, na tukaja Kadeshi ya Barnea. [20] Niliwambia, mmekuja kwenye
nchi ya milima ya Amorites, ambayo Yahwe Mungu wetu anatupa sisi. [21] Tazama,
Yahwe Mungu wenu amekwisha weka nchi mbele yenu; nenda juu, muimiliki, kama
Yahwe, Mungu wa baba zenu, amekwisha zungumza nanyi, msiogope wala kukata
tamaa. [22] Kila moja wenu alikuja kwangu na kusema, 'Basi tutume watu mbele
yetu, ili kwamba waweze kupepeleza nchi kwa ajili yetu, na kutuletea sisi neno
kuhusiana na njia ya wapi tuvamie, na kuhusiana na miji tutakayoingia. [23] Shauri
hilo lilinibariki mimi, 'Nilichukua watu kumi na mbili kutoka kwenu, mtu moja
kwa kila kabila. [24] Waligeuka na kwenda juu ya nchi ya milima, kufika kwenye
bonde la Eshcol na kufanya upepelezi wa kina. [25] Walichukua baadhi ya mazao ya
ardhi mikononi mwao na kuleta kwetu, Pia walileta neno na kusema, 'Ni nchi nzuri
ambayo Yahweh Mungu wetu anatupa sisi' [26] Bado mlikataa kushambulia, lakini

mliasi dhidi ya amri ya Yahwe Mungu wenu. 27 Mlilalamika katika mahema yenu
na kusema, "Ni kwa sababu Yahwe alituchukia sisi kwa kuwa ametutoa katika nchi
ya Misri, kuteweka katika mikono ya Amorites kutuangamiza. 28 Tuende wapi sasa?
Ndugu zetu wamefanya mioyo yetu kuyeyuka, kusema, Hao watu ni wakubwa na
warefu zaidi yetu, miji yao ni mikubwa na imeimarishwa kwenda mbinguni; zaidi
ya yote, tumewaona wana wa Anakim huko" 29 Kisha nikasema nao, msitishwe wala
msiwaogope. 30 Yahwe Mungu wenu, ambaye aenda mbele yenu, atawapigania, kama
yote aliyofanya kwa ajili yenu huko Misri mbele ya macho yenu, 31 na pia katika
jangwa, ambapo mmekwisha muona Yahwe Mungu wenu jinsi alivyowabeba, kama
mtu abebavyo mtoto wake, kokote mlikoenda mpaka kufika hapa.' 32 Bado licha
ya neno hili hakumwamini Yahwe Mungu wenu, 33 aliyeenda mbele yenu kwenye
njia kutafuta eneo kwa ajili yenu kuweka kambi, katika moto kwa usiku, katika
mawingu kwa mchana. 34 Yahwe alisikia sauti ya maneno yenu na alikasirika; aliapa
na kusema, 35 Hakika hakuna mmoja ya hawa watu wa kizazi hiki kiovu wataona
nchi nzuri ambayo niliapa kuwapa babu zao, 36 kasoro Kalebu mwana wa Jephuneeh;
yeye ataiona. Yeye nitampa nchi ambayo amekwisha kuikanyanga, na watoto wake,
kwa sababu alimfuata Yahwe kwa ukamilifu.' 37 Pia Yahweh alinikasirikia mimi
kwa sababu yenu, kusema, 'Wewe pia hautaingia huko, 38 Yoshua mwana wa Nuh,
ambaye amesimama mbele yako, yeye ataingia, mtie moyo, kwani yeye atawaongoza
Israeli kuimiliki. 39 Zaidi ya yote, watoto wenu wadogo, ambao mlisema watakuwa
waathirika, ambao leo hawana elimu ya uzuri au ubaya-wataenda ndani huko.
Wao nitawapa nchi hiyo, na wataimiliki. 40 Lakini ninyi, geuka na muuanza safari
kwenda jangwani kwa kuambaa njia ya bahari ya mianzi'. 41 Kisha mlinijibu na
kusema kwangu, 'Tumetenda dhambi dhidi ya Yahwe, tutaenda juu na kupigana,
tutafuata yote ambayo Yahwe Mungu wetu ametuamuru sisi kufanya'. Kila mtu
miongoni mwenu aliweka silaha za vita, na mlikuwa tayari kuvamia nchi ya milima.
42 Yahwe alisema nami, 'Waambie, msivamie na kupigana, kwa kuwa sitakuwa
pamoja nanyi, na mtashindwa na adui zenu'. 43 Nilizungumza nanyi kwa njia hii,
lakini hamkunisikiliza, Mliasi dhidi ya amri ya Yahwe, mlikuwa wenye kiburi na
mlivamia nchi ya milima. 44 Lakini Amorites, ambayo waliishi katika nchi hiyo
ya milima, walitoka dhidi yenu na kuwafukuza kama nyuki, na kuwapiga chini
huko Seir, mbali kama Hormah. 45 Mlirudi na kulia mbele ya Yahwe; lakini Yahwe
hakusikiliza sauti zenu, wala hakuwa makini kwenu. 46 Kwa hiyo mlibaki Kadeshi
siku nyingi, siku zote mlibaki huko.

# 2

1 Kisha tuligeuka na kuanza safari kuelekea jangwani kwa njia ya Bahari ya Mianzi,
kama Yahwe alivyosema nami, tulienda kuzunguka mlima wa Seir kwa siku nyingi.
2 Yahwe alizungumza nami, kusema, 3 Mmeuzungunga mlima huu kwa muda mrefu;
geukeni kaskazini. 4 Waamuru watu, kusema, "Mtapita kupitia mpaka wa ndugu
zenu, wazao wa Esau, ambao wanaishi Seir; watawaogopa ninyi. Kwa hiyo muwe
makini 5 msipigane nao, kwa kuwa sitawapa nchi yoyote yao, hapana, hakuna hata
vya kutosheleza unyao wa mguu kukanyanga, kwa kuwa nimekwisha mpa Esau
Mlima wa Seir kama miliki. 6 Mtanunua chakula kutoka kwao kwa pesa, ili kwamba
muweze kula, pia mtanunua maji kutoka kwao kwa pesa, ili kwamba muweze
kunywa. Kwa kuwa 7 Yahwe Mungu wenu amewabariki katika kazi za mikono
yenu, amejua kutembea kwenu kupitia jangwa hili kuu. Kwa hii miaka arobaini
Yahwe Mungu wenu amekuwa pamoja nanyi, na hamjapungukiwa chochote. 8 Basi
tulipita karibu na ndugu zetu, wa wazao wa Esau, ambao wanaishi Seir, mbali na
barabara la Arabah, kutoka Elathi, na kutoka Ezioni Geber. Na tuligeuka na kupita

karibu na jangwa la Moabu. 9 Yahweh aliniambia mimi,'Usiisumbue Moabu, na
usipigane nao katika vita. Kwa kuwa sitakupa nchi yake kwa miliki yako, kwa
sababu nimewapa Ar wazao wa Lot, kuwa miliki yao'. 10 (Hapo awali waliishi Waemi,
watu kama wakuu, wengi, na warefu kama Waanaki; 11 hawa pia wanafikiriwa
kuwa Rephaimu, kama Waanaki, lakini Wamoabi huwaita Waemi. 12 Wahori pia
waliishi hapo awali Seiri, lakini wazao wa Esau waliwafuata. Waliwaharibu kutoka
mbele yao na kuishi katika eneo lao, kama Israeli ilivyofanya kwa nchi ya umiliki
wake ambayo Yahwe aliwapa.) 13 "Sasa inuka na uende kwenye kijito cha Zeredi".
Kwa hiyo tulienda kwenye kijito cha Zeredi. 14 Sasa tangu siku ambapo tulikuja
kutoka Kadesh Barnea mpaka tukavuka kijito cha Zeredi, ilikuwa miaka thelathini
na nane. Ilikuwa kwa wakati huo kizazi chote cha watu waliofaa kupigana walikuwa
wamekwisha ondoka kwa watu, kama Yahwe alivyokuwa ameapa kwao. 15 Zaidi ya
yote, mkono wa Yahwe ulikuwa kinyume na kizazi hicho ili kuweza kuwaangamiza
kutoka kwa watu mpaka walipoondoka. 16 Basi ilitokea, wakati watu wote waliofaa
kwa kupigana walikuwa wamekufa, na kutoweka miongoni mwa watu, 17 kwamba
Yahwe alizungumza nami, kusema, 18 Leo mtavuka Ar, mpaka wa Moabu. 19 Wakati
mtakapofika karibu na mkabala wa watu wa Ammoni, msiwasumbue au kupigana
nao, kwa kuwa sitawapa nchi yoyote ya watu wa Ammoni kama miliki, kwa
sababu nimekwisha wapa wazao wa Lutu kama miliki". 20 (Hiyo tena ilifikiriwa
kuwa nchi ya Rephaimu. Warephaimu waliishi hapo awali-lakini Wammonites
wanawaita Zamzummim, 21 watu kama wakuu, wengi, na warefu kama Anakim.
Lakini Yahwe aliwaharibu mbele ya Wammonites na waliwafuata na kuishi katika
maeneo yao. 22 Yahwe huyu pia alifanya kwa watu wa Esau ambao wanaishi Seiri,
wakati alipowangamiza Wahori kutoka mbele yao, na wazao wa Esau waliwafuata na
waliishi katika maeneno yao mpaka leo. 23 Na Waavi, walioishi katika vijiji vya mbali
ya Gaza, Wakaftori, ambao wanatokana na Kaftori, waliwangamiza na kuishi katika
maeneo yao.) 24 Sasa inuka, nenda njia yako na uvuke bonde la Arnoni, tazama,
nimekupa mkononi mwako Sihoni ya Amorite, mfalme wa Heshboni, na nchi yake.
Anza kuimiliki na pigana naye katika vita. 25 Leo nitaanza kuweka woga na hofu
yenu kwa watu ambao wako chini ya anga lote, watasikia habari kuhusu ninyi na
watatemeka na kuwa na shida kwa sababu yenu'. 26 Nilituma wajumbe toka jangwa
la Kedemothi kuelekea Sihoni, mfalme wa Heshbon, pamoja na maneno ya amani,
kusema, 27 Hebu nipite katika nchi yako; nitapita kwenye barabara kuu, sitageuka
mkono wa kulia wala kushoto. 28 Mtaniuzia mimi chakula kwa pesa, ili kwamba
niweze kula, nipe maji kwa pesa, ili kwamba niweze kunywa, peke niruhusu kupitia
kwa miguu yangu, 29 kama wazao wa Esau wanaoishi Seiri, na Moabu wanaoishi
Ari, walifanya kwangu, mpaka nivuke Yordani ndani ya nchi ambayo Yahwe Mungu
wetu anatupa sisi'. 30 Lakini Sihon, mfalme wa Heshbon, asingeturuhusu kupitia
kwake; kwa kuwa Yahwe Mungu wenu ameifanya ngumu akili yake na kufanya
moyo wake kuwa ukaidi, ili kwamba aweze kumshinda kwa nguvu zake, ambayo
amekwisha kufanya leo. 31 Yahwe alisema kwangu, "tazama, Nimeanza kumuokoa
Sihoni na nchi yake mbele yako; kuanza kuimiliki, ili kusudi muweze kumiliki nchi
yake. 32 Kisha Sihon alikuja dhidi yetu, yeye na watu wote wake, kupigana huko
Jahazi. 33 Yahwe Mungu wetu alimtoa kwetu na tulimshinda, tulimpiga mpaka kufa,
watoto wake, na watu wake wote. 34 Tulichukua miji yake yote kwa wakati huo
na kuharibu kabisa kila mji- wanaume na wanawake na watoto wadogo; hatukuacha
aliyenusurika. 35 Ng'ombe peke tulichukua kama mateka kwa ajili yetu, sambamba na
mateka ya miji tuliochukua. 36 Kutoka Aroer, ambayo iko kwenye ukingo wa bonde la
Arnon, na kutoka kwenye mji ambao uko bondeni, yote kwa njia ya kuelekea Galeadi,
hapakuwa na mji uliokuwa mrefu kwetu. Yahwe Mungu wetu alitupa ushindi dhidi

ya maadui zetu mbele yetu. [37] Ilikuwa nchi ya wazao wa Ammoni peke yake ambayo hamkuingia, sambamba na sehemu zote za mto Jabboki, na miji ya nchi ya milima-popote pale Yahwe Mungu wetu ametukataza sisi kwenda.

# 3

[1] Kisha tuligeuka na kwenda njia ya juu Bashani. Ogi, mfalme wa Bashani, alikuja
na kutuvamia, yeye na watu wake wote, kupigana huko Edrei. [2] Yahwe aliniambia
mimi, "Usimuogope; kwa kuwa nimekupa ushindi dhidi yake na nimewaweka watu wake wote na nchi yake chini ya utawala wako. Utamfanya kama ulivyomfanya
Sihoni, mfalme wa Amorites, aliyeishi Heshbon. [3] Kwa hiyo Yahwe Mungu wetu pia
alitupa ushindi dhidi ya Ogi mfalme wa Bashani, na watu wake wote waliwekwa chini ya utawala wetu. Na tulimpiga mpaka kufa na hakuna yoyote wa watu wake
walibaki. [4] Tulichukua miji yake yote kwa wakati huo; hapakuwa na mji hata mmoja ambao hatukuchukua kutoka kwao: miji sitini - mikoa ya Argobi yote, ufalme wa Ogi
Bashani. [5] Hii ilikuwa miji iliyoimarishwa na kuta ndevu, malango, na vizuizi, hii
ilikuwa licha ya vijiji vingi sana vilivyokuwa havina kuta. [6] Tuliviangamiza kabisa,
kama tulivyofanya kwa Sihoni mfalme wa Heshbon, kabisa tuliangamiza kila mji-wanaume na wanawake na watoto wadogo. [7] Lakini ng'ombe wote na mateka ya
miji, tilichukua kama mateka wetu. [8] Kwa wakati huo tulichukua nchi kutoka kwenye
mkono wa wafalme wawili wa Amorites, waliokuwa ng'ambo ya pili ya Yordani,
kutoka kwenye bonde la Arnon kwenda mlima wa Hermoni, [9] (Mlima wa Hermoni,
Wasidonia huita Sirioni, na Wamorites huita Seniri) [10] na miji yote ya tambarare, yote
Gileadi, na yote Bashani kupita njia yote ya Salekah na Edrei, miji ya ufalme wa Ogi
huko Bashani". [11] (Kwa mabaki ya Refaimu, mfalme Ogi pekee wa Bashani alikuwa
amebaki. Tazama! Kitanda chake kilikuwa cha chuma. Hakuna huko Rabbah, ambako wazao wa Ammoni waliishi? Ilikuwa dhiraa tisa urefu na dhiraa nne upana,
hiyo njia walitumia watu kupima.) [12] "Hili eneo ambalo tulichukua kumiliki kwa
wakati huo-kutoka Aroer, kwamba ni kwa bonde la Arnon, na nusu ya nchi ya mlima wa Gileadi, na miji yake-Nilimpa Reubenites na kwa Gadites. [13] Waliobaki
wa Gileadi na Bashani yote, ufalme wa Ogi, Niliwapa nusu kabila la Manasseh: kwa wote wa Argob, na Bashani yote. (Eneo hilo linaitwa nchi ya Refaim) [14] Jair, mzao
wa Manasseh, alichukuwa mkoa wote wa Argob, kuelekea mpaka wa Geshunites na wa Maacathites. Aliita mkoa hata Bashani kwa jina lake, Havvothi Jair, hadi
leo.) [15] Nilimpa Gileadi kwa Machir. [16] Kwa Reubenites na kwa Gadites nilitoa eneo
kutoka kwa Gileadi kuelekea bonde la Arnon- katikati mwa bonde ni mpaka wa eneo-na kuelekea mto wa Jabbok, ambao umepakana ni wazao wa Ammoni. [17] Moja ya
mipaka mingine pia ni tambarare ya bonde la mto wa Yordani, kutoka Chinnerethi kuelekea bahari ya Arabah(ambayo ni bahari ya Chumvi) kuelekea miteremko wa
mlima wa Pisgah mashariki. [18] Nilikuamuru wewe kwa wakati huo, kusema, Yahwe
Mungu wako amekupa nchi hii kuimiliki, wewe, wamaume wote wa vita, watapita
wakiwa na silaha mbele ya ndugu zako, watu wa Israeli. [19] Lakini wake zenu, watoto
wenu, na ng'ombe zenu (najua ya kuwa una ng'ombe wengi) watabaki katika miji
yenu niliyowapa, [20] mpaka Yahwe awape pumziko ndugu zenu, kama alivyo kwenu,
mpaka wamiliki pia nchi ambayo Yahwe Mungu wenu anawapa ng'ambo ya pili Yordani, kisha mtageuka, kila mtu wenu, kwa mali zenu ambazo nimekwishawapa.
[21] Nilimwamuru Yoshua kwa wakati huo, kusema, 'Macho yenu yameona yote yale
Yahwe Mungu wenu amefanya kwa hawa wafalme wawili; Yahwe atafanya hivyo
kwa falme zote kote mtakakoenda. [22] Hamtawaogopa, kwa kuwa Yahwe Mungu
wenu ndiye atakaoawapigania.' [23] Nilimsihi Yahwe kwa wakati huo, kusema, [24] 'O
Bwana Yahwe, umeanza kumuonesha mtumwa wako ukuu wako na mkono wako wa

hodari; kwa kuwa nani mungu aliyeko huko mbinguni au duniani ambaye anaweza
kufanya kazi zilezile kama ilivyofanya, na matendo yaleyale makuu? 25 Hebu niende
juu, Ninakuoma, na nione nchi nzuri ambayo ng'ambo ya pili ya Yordani, ile nchi
nzuri ya mlima, na pia Lebanoni. 26 Lakini Yahwe alikuwa amenikasirikia mimi kwa
sababu yenu, hakunisikiliza mimi. Yahwe alisema kwangu, "Hebu hii iwe ya kutosha
kwako - usizungumze zaidi tena kwangu kuhusu jambo hili. 27 nenda juu ya kilele
cha Pisgah na uinue macho yako magharibi, mashariki, kusini na mashariki; tazama
kwa macho yako kwa kuwa hautaenda zaidi ya Yordani. 28 Badala yake, mwelekeze
Yoshua na kumtia moyo na kumuimarisha, kwa kuwa ataenda zaidi mbele ya watu,
na atawasababisha kuirithi nchi ambayo mtaiona. 29 Kwa hiyo tulibaki katika bonde
mkabala mwa Beth Peor.

# 4

1 Sasa, Israeli, sikiliza sheria na amri ambayo niko karibu kukufundisha, kuzifanya,
ili kwamba uweze kuishi na kuingia ndani na kumiliki nchi ambayo Yahwe,
Mungu wa baba zako, anakupa. 2 Hautaongeza maneno ambayo nakuamuru, wala
hautayapunguza, ili kwamba uweze kushika amri ya Yahwe Mungu wako ambazo
naenda kukuamuru. 3 Macho yako yamekwisha ona nini Yahwe alifanya kwa sababu
ya Baal Peor, kwa kuwa watu wote waliomfuata Baali Peor, Yahwe Mungu wenu
amekwisha kuwaangamiza kutoka miongoni mwenu. 4 Lakini walioambatana na
Yahwe Mungu wenu wako hai leo, kila moja wenu. 5 Tazama, nimewafundisha sheria
na amri, kama Yahwe Mungu wangu alivyoniamuru mimi, ila kwamba mfanye hivyo
katikati mwa nchi ambayo mnaiendea ili kusudi muimiliki. 6 Kwa hiyo washikilieni
na kuwafanya, kwa kuwa hii ni hekima yenu na uelewa wenu mbele ya macho ya
watu watakaosikia amri hizi zote na kusema, "Hakika taifa hili kubwa lina watu
wa hekima na uelewa.' 7 Kuna taifa gani jingine la vile liko hapo lina mungu
karibu nao, kama Yahwe Mungu wetu tunapomwita wakati wowote? 8 Kuna taifa
kubwa gani jingine liko hapo ambalo lina sheria na amri ili kwamba haki pamoja
na sheria ambayo ninaweka mbele yenu leo? 9 Zingatia peke na kuwa makini
kujilinda, ili usisahau mambo ambayo macho yako yameona, ili kwamba yasiuwache
moyo wako kwa siku zote za maisha yako. Badala yake, yafanye yajulikane kwa
watoto wako na wana watoto wako. 10 Kuhusu siku ile uliyosimama mbele ya
Yahwe Mungu wako katika Horeb, wakati Yahwe alisema nami, 'Nikusanyie watu, na
nitawafanya wasikia maneno yangu, ili kwamba waweze kujifunza kuniogopa mimi
siku zote ambazo wanazoishi duniani, na kwamba waweze kuwafundisha watoto
wao. 11 Mlikuja karibu na kusimama katika wayo wa mlima. Mlima uliwaka moto
kwenye moyo wa mbinguni, pamoja na giza, mawingu na giza jembamba. 12 Yahwe
alizungumza katikati ya moto, ulisikia suati pamoja na maneno yake, lakini hakuona
umbo, ila ulisikia sauti peke. 13 Alitangaza kwenu agano lake ambalo aliwaamuru
ninyi kulifanya, amri kumi. Aliziandika kwenye vibao viwili vya mawe. 14 Yahwe
aliniamuru mimi kwa wakati huo kuwafundisha sheria na amri, ili kwamba muweze
kuzifanya katika nchi mnaoivuka kwenda kuimiliki. 15 Basi iweni waangalifu ninyi
wenyewe - kwa kuwa mliona hakuna namna ya umbo siku hiyo ambapo Yahweh
alizungumza nanyi huko Horeb kutoka katikati mwa moto, 16 ili kwamba usiharibike
na kuchonga umbo katika sura ya kiumbe chochote, umbo la mwanaume au mtu
wa kike, 17 au sura ya mnyama aliye katika nchi, au sura ya ndege yoyote wa
mabawa arukae katika anga, au 18 sura ya kitu chochote kitambaacho katika ardhi,
au sura ya samaki yoyote katika maji chini ya ardhi. 19 Hautainua macho yako juu
mbinguni na kutazama jua, mwezi, au nyota - jeshi lote la mbinguni- ukusogezwa na
kuviabudu na kuvisujudia- vile vyote ambavyo Yahwe Mungu wenu amewapa hisa

watu wote walio chini ya anga lote. [20] Lakini Yahwe amewatoa ninyi na kuwaleta
nje ya tanuru la chuma, nje ya Misri, kuwa kwake watu wa urithi wake, kama
mlivyo leo. [21] Yahwe alinikasirikia mimi kwa sababu yenu; aliapa kwamba nisiende
ng'ambo ya Yordani, na kwamba nisiende kwenye nchi nzuri, nchi ambayo Yahwe
Mungu wenu anawapa ninyi kama urithi. [22] Badala yake, ninapaswa kufa katika
nchi hii, sipaswi kwenda ng'ambo ya Yordani, lakini mtaenda ng'ambo na kuimiliki
nchi nzuri [23] Zingatia ninyi wenyewe, ili kwamba msisahau agano la Yahwe Mungu
wenu, alilolifanya pamoja nanyi, na kujichongea mfano wa sanamu katika uombo
la kitu chochote ambacho Yahwe Mungu wenu amewakataza kufanya. [24] Kwa kuwa
Yahwe Mungu wenu ni moto ulao, Mungu wa wivu. [25] Wakati mnapozaa watoto
na wana watoto, na wakati mtakapo kuwa katika nchi kwa muda mrefu, na kama
mtaharibikiwa ninyi na kuchonga umbo la umbo lolote, na kufanya uovu machoni pa
Yahwe Mungu wenu, kumchoche katika hasira- [26] Nitaita nchi na mbingu kushuhudia
dhidi yenu leo kwa kuwa mapema kabisa mtaangamia kutoka katika nchi ambayo
mnaiendea huko ng'ambo ya Yordani kuimiliki, hamtazidisha siku zenu ndani yake,
lakini mtaangamizwa kabisa. [27] Yahwe atawatawanyisha ninyi miongoni mwa watu,
na mtabaki wachache ki-idadi miongoni mwa mataifa, ambapo Yahwe atawaongoza
mbali. [28] Huko mtatumikia miungu mingine, kazi ya mikono ya watu, mbao na
mawe, ambayo wala haioni, kusikia, wala kunusa. [29] Lakini kuanzia hapo mtamtafuta
Yahwe Mungu wenu, na mtampata, wakati mtakapomtafuta kwa moyo wenu wote
na roho zenu zote. [30] Wakati mnakuwa katika dhiki, na wakati haya yote yatakuwa
yamekuja kwenu, katika siku za badae mtamrudia Yahwe Mungu wenu na kusikia
sauti yake. [31] Kwa kuwa Yahwe Mungu wenu ni Mungu wa rehema; hatawaangusha
wala kuwaangamiza ninyi, wala kusahau agano la baba zenu ambalo aliapa kwao.
[32] Kwa ajili ya kuuliza sasa kuhusu siku zilizopita ambazo zilikuwa mbele yenu:
tangu siku ile ambayo Mungu alimuumba mtu katika nchi, kutoka pande moja ya
mbingu hadi nyingine, uliza kama kumekuwepo chochote kama hiki kikubwa, au
chochote kama hicho imewahi kusikiwa? [33] Ilishawahi kutokea watu kusikia sauti
ya Mungu kuongea katikati ya moto, kama mlivyosikia, na kuishi? [34] Au Mungu
ameshawahi kujaribu kwenda na kujichukulia kwa ajili yake taifa kutoka miongoni
mwa taifa, kwa majaribu, ishara na maajabu na kwa vita, na mkono wa nguvu, na
mkono ulionyoshwa, na magaidi wakuu, vile vyovyote ambavyo Yahwe Mungu wenu
alifanya kwa ajili yenu Misri mbele ya macho yenu? [35] Kwenu haya yalioneshwa, ili
muweze kujua kuwa Yahwe ni Mungu, na kwamba hakuna mwingine zaidi yake.
[36] Toka mbinguni alifanya msikie sauti yake, ili kwamba aweze kuwaelekeza, juu
ya nchi aliwafanya muone moto wake mkuu, mlisikia maneno yake toka katikati ya
moto. [37] Kwa sababu aliwapenda baba zenu, alichagua wazao wao baada yao, na
kuwatoa ninyi Misri kwa uwepo wake, kwa nguvu yake kubwa, [38] ili kusudi awatowe
kutoka mbele ya mataifa makubwa na yenye nguvu kuliko ninyi, kuwaleta ndani,
kuwapa ninyi nchi yao kama urithi, hivi leo. [39] Tambua hivi leo, weka kwenye moyo
wako, Yahwe ni Mungu juu ya mbingu na chini ya dunia, hakuna mwingine yeyote.
[40] Mtazishika sheria zake na amri zake ambazo nawaamuru leo, ili kwamba iweze
kuwa vizuri kwenu na watoto wenu baada yenu, na kwamba muweze kuongeza
siku zenu katika nchi ambayo Yahwe Mungu wenu amewapa milele." [41] Kisha
Musa alichagua miji mitatu mashariki mwa Yordani, [42] ili kwamba yoyote aweze
kukimbia kati ya moja yao kama imemuua mtu mwingine kwa ajili, pasipo kuwa
adui hapo awali. Kwa kukimbilia kwenye moja ya miji hii, atakuwa amenusurika.
[43] Walikuwa: Bezeri katika jangwa, nchi tambarare, kwa Warubenites; Ramothi huko
Gileadi, kwa Gadites; na Golani huko Bashani, kwa Manassites. [44] Hii ni sheria
ambayo Musa aliweka mbele ya watu wa Israeli, [45] hizi ni amri za agano, sheria,

na amri zingine alizungumza na watu wa Israeli wakati walipotoka Misri, [46] pindi
walikuwa Mashariki mwa Yordani, katika bonde mkabala wa Beth Peori, katika nchi
ya Sihoni, mfalme wa Amorites, aliyewahi kuishi Heshbon, ambaye Musa na watu
wa Israeli waliwahi kumshinda wakati walipotoka Misri. [47] Walichukua nchi yake
kama urithi, na nchi ya Ogi mfalme wa Bashani- hawa, wafalme wawili wa Amorites,
waliokuwa ng'ambo ya pili ya Yordani kuelekea Mashariki. [48] Himaya hii ilienda
kutoka Aroer, katika ukingo wa bonde la Arnon, kwa mlima wa Sion (mlima Hermon),
[49] na ilijumuisha tambarare zote za bonde la mto Yordani, Mashariki mwa ng'ambo
ya pili ya Yordani, kuelekea bahari ya Arabah, kuelekea miteremko ya mlima Pisgah.

# 5

[1] Musa aliwaita Israeli yote na akasema nao, “Sikiliza, Israeli, kwa amri na sheria
ambazo nitasema katika masikio yenu leo, muweze kujifunza na kuzishika. [2] Yahwe
Mungu wetu alifanya agano nasi huko Horeb. [3] Yahwe hakufanya agano hili pamoja
na mababu zetu, lakini na sisi, sisi wote tu hai hapa leo. [4] Yahwe alizungumza
nawe uso kwa uso kwenye mlima toka katikati mwa moto [5] (Nilisimama kati ya
Yahwe na wewe kwa wakati huo, kukufunulia wewe neno lake, kwa kuwa ulikuwa
umeogopa kwa sababu ya moto, na haukwenda juu ya mlima), Yahwe alisema, [6] 'Mimi
ni Yahweh Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, kutoka nyumba ya utumwa.
[7] Hautakuwa na miungu mingine mbele yangu. [8] Hautajifanyia mwenyewe sanamu
ya kuchonga wala mfano wa kitu chochote kilicho juu mbinguni, au kilicho chini
ya dunia, au kilicho chini ya maji. [9] Hautavisujudia au kuvitumikia, kwa kuwa
Mimi, Yahwe Mungu wako, ni Mungu wa wivu, Nawaadhibu uovu wa mababu kwa
kuleta adhabu juu ya watoto, kwa kizazi cha tatu na cha nne cha wale wanichukiao,
[10] na kuonesha agano la uaminifu kwa maelfu, kwa wale wanaonipenda na kushika
amri zangu. [11] Hautalichukua jina la Yahwe Mungu wako bure, kwa kuwa Yahwe
hatamshikilia kuwa ana hatia yeye alichukuae jina bure. [12] Zingantia siku ya Sabato
kwa kuiweka takatifu, kama Yahwe Mungu wako alivyokuamuru. [13] Kwa siku sita
utafanya kazi na fanya kazi zako zote, [14] lakini siku ya saba ni Sabato kwa Yahwe
Mungu wako. Kwa siku hiyo hautafanya kazi yoyote- si wewe, wala mwana wako,
wala binti yako, wala mjakazi wako wa kiume, wala maksai wako, wala punda wako,
wala mifugo wako, wala mgeni yeyote aliye katika malango yako. Hii ni kwamba
mjakazi wako wa kiume na mjakazi wako wa kike wapate kumpuzika pamoja na
wewe. [15] Utakumbuka katika akili yako kwamba ulikuo mtumwa katika nchi ya
Misri, na Yahwe Mungu wako alikutoa kutoka huko kwa mkono wa uweza na mkono
ulionyoshwa. Kwa hiyo Yahwe Mungu wako amekuamuru kuitunza siku ya Sabato.
[16] Mheshimu baba yako na mama yako, kama Yahwe Mungu wako alivyokuamuru
kufanya, ili kwamba uweze kuishi muda mrefu katika nchi ambayo Yahwe Mungu
wako akupa, ili kwamba iende kwa uzuri kwako. [17] Hautaua, [18] hautazini, [19] hautaiba,
[20] hautashuhudia uongo dhidi ya ndugu yako. [21] Hautamtamani mke wa jirani yako,
hautatamani nyumba ya jirani yako, shamba lake, au mjakazi wake wa kiume, au
mjakazi wake wa kike, maksai au punda wako, au chochote ambacho ni mali ya
jirani yako. [22] Haya maneno Yahwe alisema kwa sauti kubwa kwa kusanyiko lako
lote kwenye mlima toka katikati mwa moto, mawingu, giza zito, hakuongeza maneno
yoyote zaidi. Na aliandika chini kwenye mbao mbili za mawe na akanipa mimi.
[23] Ilipokaribia, pindi uliposikia sauti toka katikati mwa giza, wakati mlima unawaka
moto, kuwa mlikuja karibu nami, wazee wako wote, na wakuu wa makibila yako.
[24] Ulisema, Tazama, Yahwe Mungu wetu ametuonesha utukufu wake na ukuu wake,
na tumeisikia sauti yake toka katikati mwa moto, tumeona leo kwamba wakati Mungu
azungumza na watu, wanaweza kuishi. [25] Lakini kwanini tufe? Kwa kuwa mto huu

mkuu utatutoshereza sisi; kama tutasikia sauti ya Yahwe Mungu wetu tena, tutakufa.
26 Kwa kuwa badala yetu kuna miongoni mwetu wa mwili ambao wamesikia sauti ya
Mungu aliye hai akizungumza toka katikati mwa moto na kuishi, kama tulivyofanya?
27 Kwenu ninyi, mnapaswa kwenda na kusikiliza kila kitu ambacho Yahwe Mungu
wetu asema; rudia kwetu kila kitu ambacho Yahwe Mungu wetu asema kwenu;
tutamsikiliza na kumtii.' 28 Yahweh alisikia maneno yenu pindi mlipozungumza
nami. Alisema na mimi, “Nimekwisha sikia maneno ya watu hawa, kile wanasema
kwako. Kile walichosema kilikuwa kizuri. 29 Oh, kulikuwa na moyo wa namba hiyo
ndani yao, kwamba wataniheshimu na daima kushika amri zangu zote, ili iweze
kuwa vizuri kwao na pamoja na watoto wao milele! 30 Nenda useme nao, “Rudini
kwenye mahema.” 31 Lakini kwenu, simama karibu nami, na nitakuambia amri zote,
sheria, na maagizo ambayo mtawafundisha, ili kwamba waweze kuyashika katika
nchi ambayo nitawapa kumiliki.' 32 Utashika, kwa hiyo, kile Yahwe Mungu wenu
amewaamuru; hamtageukia mkono wa kulia au kushoto. 33 Mtatembea katika njia
zote ambazo Yahwe Mungu wenu, amewaamuru ili kusudi muweze kuishi, na ili
kwamba iweze kwenda vizuri kwenu, na kwamba muweze kuongeza siku zenu katika
nchi ambayo mtaimiliki.

# 6

1 Sasa haya ni maagizo, amri, na sheria ambazo Yahwe Mungu wetu ameniamuru
mimi kuwafundisha ninyi, ili kwamba muweze kuzishika katika nchi ambayo
mnaenda ng'ambo ya pili ya Yordani kumiliki, 2 ili kwamba mpate kumheshimu
Yahwe wenu, ili muzishike amri zake zote na maagizo ninayowaamuru-ninyi, wana
wenu na wana wa wana wenu, siku zenu zote za maisha, ili kwamba siku zenu
ziongezeke. 3 Kwa hiyo wasikilizeni, Israeli, na kuzishika ili kwamba iweze kuwa
vizuri kwenu, ili kusudi muweze kuzidi mno kwenye nchi itiririkayo maziwa na
asali, kama Yahwe Mungu wa Baba zenu, amewaahidi atafanya. 4 Sikiliza, Israel:
Yahwe Mungu wetu ni mmoja. 5 Mtampenda Yahwe Mungu wenu kwa moyo wenu
wote, kwa roho zenu zote, na kwa akili zenu zote. 6 Maneno ninayowaamuru ninyi
leo yatakuwa katika moyo wenu; 7 na mtayafundisha kwa bidii kwa watoto wenu,
mtayazungumza wakati mkaapo katika nyumba zenu, wakati mlalapo, na wakati
mwinukapo. 8 Utazifunga kama ishara juu ya mkono wako, nayo yatakuwa utepe
kati ya macho yako. 9 Utaziandika kwenye miimo ya mlango ya nyumba yako
na kwenye malango. 10 Wakati Yahwe Mungu wako akuleta kwenye nchi ambayo
aliaapa kwa baba zako, Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, kwamba angekupa, pamoja na
miji mikubwa na mizuri ambayo hamkuijenga, 11 na nyumba zilizojaa kila aina ya
vitu vizuri ambavyo hamkuzifanya, visima ambavyo hamkuvichimba, mashamba
na miti ya mizeituni ambayo hamkuipanda, mtakula na kutosheka- 12 basi iweni
makini ili kwamba msije kumsahau Yahwe, aliyewaleta toka nchi ya Misri, toka
nyumba ya utumwa. 13 Mtamheshimu Yahwe Mungu wenu, yeye mtamwabudu,
na mtaapa kwa jina lake. 14 Hamtawaendea miungu mingine, miungu ya watu
wanaowazunguka wote- 15 kwa kuwa Yahwe Mungu wenu katikati yenu ni Mungu
wa wivu- kama mtafanya, hasira ya Yahwe Mungu wenu atawasha dhidi yenu na
atawaangamiza kutoka kwenye uso wa dunia. 16 Hamtamjaribu Yahwe Mungu wenu
kama mlivyomjaribu huko Massah. 17 Kwa bidii mtayashika maagizo ya Yahwe
Mungu wenu, maagizo yake makini, na amri ambazo amewaamuru. 18 Mtafanya
kile kilicho sahihi na kizuri katika macho ya Yahwe, kwamba iwe vizuri kwenu,
na kwamba muweze kuingia na kumiliki nchi nzuri ambayo Yahwe aliaapa kwa
baba zenu, 19 kuwaondoa maadui zenu wote mbele zenu, kama Yahwe alivyosema.
20 Wakati mwana wako auliza kwa wakati unaokuja, kusema,”Ni zipi amri za gano,

sheria, na amri zingine ambazo Yahwe Mungu wetu alituamuru? [21] Basi utasema
kwa mwana wako, tulikuwa watumwa wa Farao huko Misri, Yahwe alitutoa Misri
kwa mkono wa uweza, [22] na alionesha ishara na maajabu, makuu na makali, Misri
kwa Farao, na kwa nyumba yake yote, mbele ya macho yenu, [23] na alitutoa kutoka
huko, ili kwamba atulete ndani, kutupa nchi ambayo aliaapa kwa baba zetu. [24] Yahwe
alituamuru daima kuzishika amri hizi, kumuogopa Yahwe Mungu wetu kwa uzuri
wetu, ili kwamba atuweke hai, kama tulivyo leo. [25] Kama tutashika maagizo haya
yote mbele ya Yahwe Mungu wetu kama alivyotuamuru, hii itakuwa haki yetu.

# 7

[1] Wakati Yahwe Mungu wenu atuleta katika nchi ambayo mnaenda kuimiliki na
kuwaondoa mataifa mengi mbele zenu- Mhiti, Mgirgashi na Mwamori, na Mkanaani,
na Mperizi, Mhivi, Myebusi- mataifa saba makubwa na yenye nguvu kuliko wewe.
[2] Na wakati Yahwe Mungu wenu awapa ninyi ushindi juu yao pindi mnakutana nao
katika vita, mtawashambulia, basi mnapaswa kuwateketeza kabisa. Hamtafanya
agano nao, wala kuonesha huruma kwao. [3] Wala hamtapanga ndoa zozote pamoja
nao, hamtawatoa binti zenu kwa vijana wao, na hamtawachukua binti zao kwa vijana
wenu. [4] Kwa kuwa watawabadilisha vijana wenu kutonifuata mimi, ili kwamba
waweze kuabudu miungu yao. Kwa hiyo hasira ya Yahwe itawashwa dhidi yenu
na atawaangamiza haraka. [5] Hivi ndivyo mtakavyo washughulikia nao; mtavunja
madhabahu zao, vunja nguzo zao za mawe katika vipande, kata chini ncha za
Asherahi, na kuzichoma sanamu za kutupwa. [6] Kwa kuwa wewe ni taifa uliyetengwa
kwa Yahwe Mungu wako. Amekuchagua wewe kuwa watu kwa ajili yake kumiliki,
zaidi ya watu wengine wote ambao wako katika uso wa dunia. [7] Yahwe hakuweka
upendo wake juu yenu au kuwachagua kwa sababu mlikuwa zaidi katika idadi kuliko
watu wowote, kwa kuwa mlikuwa wachache kuliko watu wote- [8] Lakini kwa sababu
anawapenda ninyi, anataka kushika kiapo alichoapa kwa baba zenu. Huyu ni Yahwe
aliyewatoa kwa mkono wa uweza na kuwakomboa kutoka nyumba ya utumwa,
kutoka mkono wa Farao, mfalme wa Misri. [9] Kwa hiyo tambua ya kuwa Yahwe
Mungu wako-ni Mungu, Mungu mwaminifu, anayetunza maagano na uaminifu kwa
vizazi elfu kwa wale wanaompenda na kuyashika maagizo yake, [10] lakini huwalipa
wale wanaomchukia kwa sura zao, kuwaangamiza, hatakuwa na huruma kwa yeyote
anayemchukia; atamlipa kwa uso wake. [11] Kwa hiyo utashika maagizo, amri, na
sheria ninazokuamuru leo, ili kwamba uzifanye. [12] Kama mtasikiliza maagizo
haya, kuyashika na kuyafanya, itakuwa Yahwe Mungu wenu atawashika pamoja
na agano na uaminifu ambao aliapa kwa baba zenu. [13] Atawapenda, atawabariki,
na kuwazidisha, pia atabariki tunda la miili yenu na tunda la ardhi yenu, nafaka
zenu, divai mpya, mafuta yenu, atazidisha mifugo na kundi lako la mifugo michanga,
katika nchi ambayo aliapa kwa baba zenu kuwapa. [14] Mtabarikiwa zaidi kuliko watu
wengine wote; hapatakuwa na mwanaume asiyekuwa na mtoto au mwanamke tasa
miongoni mwenu au miongoni mwa mifugo. [15] Yahwe atawaondolea magonjwa yote;
hakuna magonjwa mabaya ya Misri ambayo mnayajua yatawekwa juu yenu, Lakini
atayaweka kwa wote wanaowachukia ninyi. [16] Mtayaondoa makundi ya watu wote
ambayo Yahwe Mungu wenu awapa ushindi, na jicho lenu halitawaonea huruma. Na
hamtaabudu miungu yao, kwa kuwa huo utakuwa mtego kwenu. [17] Kama mtasema
kwenye mioyo, Haya mataifa ni mengi zaidi kuliko mimi; nitawezaje kuwafukuza?
[18] Usiwaogope; utakumbuka akilini Yahwe nini Mungu wenu alifanya kwa Farao na
Misri yote? [19] Mateso makuu ambayo macho yenu yaliona, ishara, maajabu, mkono
wa uweza, mkono ulionyoshwa ambao Yahwe Mungu wenu alivyowatoa. Yahwe
Mungu wenu atafanya kile kile kwa watu wote ambao mnawaogopa. [20] Zaidi ya

yote, Yahwe Mungu wenu atatuma nyigu miongoni mwao, mpaka wale waliobaki
na wale wanaojificha wenyewe mbele yenu waangamizwa mbele ya uwepo wenu.
21 Hamtatishikeni nao, kwa kuwa Yahwe Mungu wenu yuko miongoni mwenu, Mungu
mkuu na wa kuogofya. 22 Yahwe Mungu wenu atayaondoa mataifa mbele zenu
kidogo kidogo. Hamtayashinda yote kwa wakati mmoja, au wanyama wa mwitu
watakuwa wengi karibu yenu. 23 Lakini Yahwe Mungu wenu atawapa ninyi ushindi
dhidi yao wakati mkutanapo vitani; atawachanganya kwa kiasi kikubwa mpaka
wameangamizwa. 24 Atawaweka wafalme wao chini ya utawala wenu, na mtafanya
jina lao kuangamia toka chini ya mbingu. Hakuna atakayeweza kusimama mbele
yenu, mpaka muwaangamize. 25 Utazichoma sanamu za kuchonga za miungu yao-
usitamani madini ya fedha au dhahabu yanayofunika na kuichukua kwa ajili yenu,
kwa sababu mkifanya, mtanaswa nayo-kwa kuwa ni chukizo kwa Yahwe Mungu
wenu. 26 Hamtaleta chukizo lolote ndani ya nyumba zenu na kuanza kuiabudu.
Mtachukizwa kabisa na kuchukia kwa kuwa imetengwa kwa ajili ya uharibifu.

# 8

1 Mnapaswa kuyashika maagizo yote ninayowapa leo, ili kwamba mweze kuishi
na kuongezeka, na kuingia na kuimiliki nchi ambayo Yahwe aliaapa kwa baba
zenu. 2 Mtakumbuka akilini njia zote ambazo Yahwe Mungu amewaongoza miaka hii
arobaini kwenye jangwa, ili kwamba apate kuwanyenyekeza, ili kwamba awajaribu
kujua nini kilikuwa ndani ya mioyo yenu, kama mungeweza kuyashika maagizo
yake au hapana. 3 Aliwanyenyekeza, na kuwafanya kuwa na njaa, na kuwalisha
manna, ambayo hamkuijua na ambayo baba zenu hawakuijua. Alifanya hivyo
kuwafanya nyie kujua si kwa mkate tu watu wanaishi, badala ni kwa chochote hutoka
kwenye kinywa cha Yahwe kwamba watu wanaishi. 4 Mavazi yenu hayakuchanika
na kudondoka, na miguu yenu haikuvimba kipindi cha miaka hiyo arobaini.
5 Mtatafakari katika mioyo yenu kuhusu, namna, kama mtu anavyo mwadibisha
kijana wake, hivyo Yahwe Mungu wenu anawadibisha ninyi. 6 Mtayashika maagizo ya
Yahwe Mungu wenu, ili kwamba mweze kutembea katika njia zake na kumheshimu.
7 Kwa kuwa Yahwe Mungu wenu anawaleta katika nchi nzuri, nchi ya vijito vya maji,
visima na chemchemi, vitiririkavyo kwenda kwenye mabonde na miongoni mwa
milima, 8 nchi ya ngano na shayiri, mizabibu, mtini, na komamanga; nchi mizeituni
na asali. 9 Ni nchi ambayo mtakula mkate bila kupungukiwa, na ambapo mtaenda
bila chochote; nchi ambayo mawe yametengenezwa kwa chuma, na kutokana na
milima mtaweze kuchimba shaba. 10 Mtakula na kushiba, na mtambariki Yahwe
Mungu wenu kwa nchi nzuri ambayo amewapa. 11 Iweni makini kwamba msimsahau
Yahwe Mungu wenu, na kwamba msipuuzie maagizo yake, hukumu zake, na
sheria zake ambazo ninakuamuru leo, 12 vinginenyo unapokula na ukashiba, na
wakati unajenga nyumba nzuri na kuishi ndani zao. 13 Na muwe makini wakati
makundi yenu na mifugo yenu ikiongezeka, na wakati wa fedha zenu na dhahabu
zenu zikiongezeka, na vyote mlivyonavyo kuongezeka, 14 basi kwamba mioyo yenu
iliniuliza juu ya kumsahau Yahwe Mungu wenu-aliyewaleta kutoka nchi ya Misri,
toka nyumba ya utumwa. 15 Usimsahau yeye aliyewaongoza kupitia jangwa kuu
na la kutisha, ambako ndani yake kulikuwa na nyoka wa moto na nge, na pitia
nchi yenye kiu ambako hapakuwa na maji, ambaye yeye alileta maji toka kwenye
mwamba wa jiwe. 16 Ambaye aliwalisha kwenye jangwa kwa manna ambayo
mababu zenu hawakuijua, ili kwamba awajaribu, kufanya uzuri kwenu mwishoni-
17 lakini mnaweza kusema mioyoni mwenu, Nguvu yangu na mkono wangu wa
uweza umepata utajiri huu wote. 18 Lakini mtamkumbuka akilini Yahwe Mungu
wenu, kwa kuwa ni yeye awapae ninyi nguvu ya kupata utajiri, ili kwamba aweze

kuanzisha agano lake aliloapa kwa baba zenu, kama ilivyo leo. [19] Itakuwa kwamba,
kama mtamsahau Yahwe Mungu wenu na kuwaendea miungu mingine, kuibudu,
na kuiheshimu, nashuhudia kinyume dhidi yenu leo kwamba mtateketea. [20] Kama
mataifa ambayo Yahwe anatengeneza kuyaangamiza mbele yenu, hivyo mtaangamia,
kwa sababu hamkusikiliza sauti ya Yahwe Mungu wenu.

# 9

[1] Sikiliza, Israeli; umekaribia kuvuka ng'ambo ya pili ya Yordani leo, kuyafukuza
mataifa yenye nguvu na ushujaa kuliko ninyi, na miji ambayo ni mikuu na yenye
boma iliyoenda juu, [2] watu wakuu na warefu, wana wa Anakimu, ambaye mnamjua,
na yule mliomsikia watu wakisema, 'Nani atasimama mbele ya wana wa Anak?
[3] Kwa hiyo tambua leo kwamba, Yahwe Mungu wenu ni yeye ambaye huenda mbele
yenu kama moto uwalao; atawaharibu na kuwaangamiza mbele yenu, kwa hiyo
mtawaondosha na kuwafanya kuwapoteza kwa haraka, kama Yahwe alivyosema
kwenu. [4] Msiseme kwenye mioyo yenu, baada ya Yahwe Mungu wenu kuwatupilia
toka mbele yenu, “ilikuwa kwa sababu ya haki yangu kwamba Yahwe ameniletа mimi
kuimiliki nchi hii; kwa kuwa ilikuwa kwa sababu ya maovu ya mataifa haya kwamba
Yahwe anawaondowa toka mbele yenu. [5] Si kwa sababu ya uadilifu wenu au unyofu
wa mioyo yenu ambayo mnaenda kuingia kumiliki nchi yao, lakini ni kwa sababu
ya maovu ya mataifa haya ambayo Mungu anawaondowa kutoka mbele zenu, na
kusudi alifanye kuwa kweli neno ambalo aliapa kwa mababu zenu, Ibrahimu, Isaka
na Yakabo. [6] Kwa hiyo tambua, kwamba Yahwe Mungu wenu awapi ninyi nchi hii
nzuri kuimiliki kwa sababu ya uadilifu wenu kwa kuwa ni watu wakaidi. [7] Kumbuka
na msisahau jinsi mlivyomchochea Yahwe Mungu wenu katika hasira huko jangwani;
kutoka siku hiyo ambayo mliacha nchi ya Misri mpaka mlipokuja kwenye eneo hili,
mmekuwa waasi dhidi ya Yahwe. [8] Pia huko Horebu mlimchochea Yahwe katika
hasira, na Yahwe alikasirika vya kutosha kwenu kuwaangamiza. [9] Wakati nilipoenda
juu ya mlima kupokea mbao za mawe, mbao za agano ambalo Yahwe alifanya nanyi,
Nilibaki kwenye mlima kwa siku arobaini na usiku arobaini; Wala sikula mkate wala
kunywa maji. [10] Yahwe alinipa mbao mbili za mawe zilizoandikwa kwa kidole chake;
juu yake kuliandikwa kila kitu kama tu maneno yote ambayo Yahwe alitangaza
kwenu juu ya mlima toka katikati mwa moto siku hiyo ya kusanyiko. [11] Ilitokea
mwishoni mwa siku hizo arobaini na usiku arobaini ya kwamba Yahwe alinipa mimi
mbao mbili za mawe, mbao za agano. [12] Yahwe alisema nami, 'Inuka, nenda chini
haraka kutokea hapa, kwa kuwa watu wako, ambao uliwaleta toka Misri, wamekuwa
wafisadi wenyewe. Kwa haraka wamegeuka toka kwenye njia ambayo niliwaamuru.
Wamejifanyia wenyewe umbo la kutupwa. [13] Zaidi ya hayo, Yahwe alizungumza
na mimi na kusema, “Nimewaona watu hawa; ni watu wakaidi. [14] Acha mimi
peke yangu, ili kwamba niweze kuwaangamiza na kulifuta jina lao kutoka chini ya
mbingu, na nitawafanya ninyi taifa lenye nguvu na kuu kuliko wao.” [15] Kwa hiyo
niligeuka nyuma na kushuka chini ya mlima, na mlima ulikuwa ukiwaka moto. Mbao
mbili za agano zilikuwa kwenye mikono yangu. [16] Nilitazama, na tazama, mlikuwa
mmefanya dhambi dhidi ya Yahwe Mungu wenu. Mmejitengenezea wenyewe
ndama. Kwa haraka mmegeuka toka njia ambayo Yahwe alikuwa amewaamuru.
[17] Nilizichukua mbao mbili na kuzitupa toka mikononi mwangu. Nilizivunja mbele
ya macho yenu. [18] Tena nilala kifudifudi mbele ya Yahwe kwa siku arobaini na
usiku arobaini; wala sikula mkate wala kunywa maji, kwa sababu dhambi zenu
zote ambazo mlikuwa mmefanya, kwa kufanya hivyo ambavyo ilikuwa ni mbaya
machoni pa Yahwe, ili kwamba kumchochea yeye katika hasira. [19] Kwa kuwa
nilikuwa nimeogopa hasira na gadhabu kali ambayo Yahwe alikuwa amekasirika

vya kutosha dhidi yenu kuwaangamiza. Lakini Yahwe alinisikiliza mimi kwa wakati
huo pia. 20 Yahwe alikuwa na hasira nyingi na Aaroni kwa kusudi la kumuangamiza;
pia niliomba kwa ajili ya Aaroni kwa wakati huohuo. 21 Nilichukua dhambi zenu,
ndama mliyekuwa mmentengeza, na kumchoma, kumpiga, kumweka chini kuwa
mdogo, mpaka ilipokuwa laini kama vumbi. Nilirusha vumbi lake katika mkondo
ambao ulitiririka chini kutoka mlimani. 22 Huko Taberah, Massah, na huko Kibrothi
Hattaavah, mlimchochea Yahwe kwenye adhabu. 23 Wakati Yahwe aliwatoa kutoka
Kadeshi ya Barnea na kusema, 'Nenda juu na umiliki nchi ambayo nimekupa, 'ndipo
mliasi dhidi ya agizo la Yahwe Mungu wenu, na hamkumwamini na kumsikiliza sauti
yake. 24 Mmekuwa waasi dhidi ya Yahwe toka siku ile nilipowajua. 25 Kwa hiyo
nilala kifudifudi mbele ya Yahwe siku zile arobaini na usiku arobaini, kwa sababu
alikuwa amesema kwamba angewaangamiza. 26 Niliomba kwa Yahwe na kusema,
'Oh Bwana Yahwe, usiwaangamize watu wako au warithi wako ambao uliwaokoa
kwa ukuu wako, ambapo uwatoa toka Misri kwa mkono wa uweza. 27 Akilini waite
watumishi wenu Ibrahimu, Isaka, na Yakobo; msiangalie ukaidi wa watu hawa, wala
maovu yao, dhambi zao, 28 ili kwamba nchi ambayo ulitutoa iseme, “Kwa sababu
Yahwe hakuweza kuwaleta katika nchi aliyowaahadia, na kwa sababu aliwachukia,
amewaleta nje kuwauwa katika jangwa. 29 Bado ni watu wa kwenu na urithi wenu,
ambao uliwatoa kwa nguvu zako kuu na kwa kuonesha mamlaka yako,

# 10

1 Kwa wakati ule Yahwe alisema kwangu, 'Chonga mbao mbili za mawe kama zile
za kwanza, na njoo kwangu huku juu ya mlima, na utengeneze sanduku la mbao.
2 Nitaandika kwenye mbao maneno ambayo yalikuwa kwenye mbao za kwanza
ulizozivunja, na utaziweka ndani ya sanduku. 3 Basi nilitengeneza sanduku la mbao
za mikaratusi, na nikachonga mbao mbili za mawe kwa zile za kwanza, na nikaenda
juu ya mlima, nikiwa na mbao mbili mkononi mwangu. 4 Aliandika kwenye mbao,
kama maandishi ya kwanza, amri kumi ambazo Yahwe amesema nanyi kwenye
mlima kutoka katikati mwa moto katika siku ya kusanyiko; ndipo Yahwe alililinipa
mimi. 5 Niligeuka na kushuka chini kutoka mlimani, na kuweka mbao ndani ya
sanduku nililokuwa nimetengeneza; hapo zilikaa, kama Yahwe alivyoniamuru.”
6 (Watu wa Israeli walisafiri kutoka Beerothi ya Bene Jaakan kwenda Moserathi.
Huko Aaroni alikufa, na huko alizikwa; Eleazar, mwana wake, alitumika katika ofisi
ya ukuhani kwenye nafasi yake. 7 Kutokea huko walisafiri kwenda Gudgodah, na
kutoka Gudgodah kwenda Jotbathah, nchi yenye mikondo ya maji. 8 Kwa wakati huo
Yahwe alichagua kabila la Lawi kubeba sanduku la agano la Yahwe, kusimama mbele
ya Yahwe kumtumikia na kubariki watu kwa jina lake, kama ilivyo leo. 9 Kwa hiyo
Lawi hawana sehemu wala urithi wa nchi pamoja na ndugu zake; Yahwe ni urithi
wao, kama Yahwe Mungu wenu alizungumza naye) 10 “Nilibaki kwenye mlima kama
ilivyokuwa mara ya kwanza, siku arobaini na usiku arobaini. Yahwe alinisikiliza
wakati huo pia; Yahwe hakutaka kukuangamiza. 11 Yahwe alisema nami, “Inuka,
nenda mbele ya watu uwaongoze katika safari yao; wataingia na kumiliki nchi
ambayo niliapa kwa mababu zao kuwapa.' 12 Sasa, Israeli, Yahwe Mungu wenu ataka
nini kwenu, isipokuwa hofu ya Yahwe Mungu wenu, kutembea katika njia zake zote,
kumpenda yeye, na kumwabudu Yahwe Mungu wenu kwa moyo wenu wote na roho
yenu yote. 13 Kuzishika amri za Yahwe, na maagizo ambayo ninawaamuru ninyi
leo kwa ajili ya uzuri wenu? 14 Tazama, kwa Yahwe Mungu wenu mbingu ni zake
na mbingu za mbingu, dunia, vyote vilivyomo. 15 Yahwe peke alichukua furaha kwa
baba zenu ili kwamba awapende, na aliwachagua ninyi, wazao wao, baada yao, zaidi
kuliko ya watu wengine wowote, kama afanyavyo leo. 16 Kwa hiyo basi wataili govi la

mioyo yao, na msiwe wakaidi tena. 17 Kwa kuwa Yahwe Mungu wenu, ni Mungu wa
miungu na Bwana wa bwana, Mungu mkuu, mwenye nguvu na wakutisha, ambaye
hapendelei yeyote na hapokei rushwa- 18 Hutekeleza haki kwa yatima na wajane,
na huonesha upendo kwa mgeni kwa kumpa chakula na mavazi. 19 Kwa hiyo basi
mpende mgeni; kwa kuwa mlikuwa wageni kutoka nchi ya Misri. 20 Mtamche Yahwe
Mungu wenu yeye mtamwabudu. Mtashikamana kwake, na kwa jina lake mtaapa.
21 Yeye ni sifa yenu, ni Mungu wenu, ambaye amefanya kwa ajili yenu haya mambo
makuu na kutisha, ambayo macho yenu yameyaona. 22 Baba zako walienda Misri
kama watu sabini; sasa Yahwe Mungu wako amekufanya wewe kuwa wengi kama
nyota za mbinguni.

# 11

1 Kwa hiyo mtampenda Yahwe Mungu wenu na daima mtashika maelekezo yake,
maagizo yake, sheria zake, na amri zake. 2 Kumbuka kwamba siongei kwa watoto
wako, ambao hawajajua wala kuona hukumu ya Yahwe Mungu wako, ukuu wake,
mkono wake wa uweza, mkono wake ulionyoshwa, 3 Ishara na matendo ambayo
alifanya katikati ya Misri kwa Farao, mfalme Misri, na nchi yake yote. 4 Wala
hawakuona kile alichofanya kwa jeshi la Misri, kwa farasi wao, au magari yao; namna
alivyoyafanya maji ya bahari ya Reeds kuwaelemea kwa sababu ya kuwafuatilia, na
namna Yahwe alivyowaangamiza mpaka leo, 5 au nini alifanya kwenu kwenye jangwa
mpaka mlikuja eneo hili. 6 Hawajaona nini Yahwe alichofanya kwa Dathani na
Abiramu, wana wa Eliabu mwana wa Reubeni; namna dunia ilifungua kinywa chake
na kuwameza, nyumba zao, mahema yao, na kila kitu hai kilichowafuata, katikati
mwa Israeli yote. 7 Lakini macho yenu yameona kazi yote kuu ya Yahwe aliyoifanya.
8 Kwa hiyo shikeni amri zote ambazo ninawaamuru leo, kwamba mweze kuwa imara,
na kuingia na kuimiliki nchi, ambayo unaenda zaidi kuimiliki; 9 na kwamba uweze
kuongeza siku zako katika nchi ambayo Yahwe aliapa kwa baba zako kuwapa na uzao
wao, nchi itiririkayo maziwa na asali. 10 Kwa kuwa nchi, ambayo unaingia kumiliki,
siyo kama nchi ya Misri, ambako mlitoka, ambako mlipanda mbegu na kumwagilizia
kwa miguu yenu, kama bustani ya mitishamba; 11 Lakini nchi, ambayo unaenda
kuimiliki, ni nchi ya milima na mabonde, na kunywa maji ya mvua mbinguni,
12 nchi ambayo Yahwe Mungu wenu awajali; macho ya Yahwe Mungu wenu daima
yako juu yake, kuanzia mwanzo wa mwaka mpaka mwisho wa mwaka. 13 Itatokea,
kama mtazisikiliza kwa bidii amri zangu ambazo ninawaamuru leo kumpenda Yahwe
Mungu wenu, na kumtumikia kwa moyo wenu wote na roho zenu zote, 14 kwamba
nitawapa mvua nchi yenu kwa majira yake, mvua za awali na mvua za badaye,
ili kwamba mweze kukusanya nafaka zenu, mvinyo wenu mpya, na mafuta yenu.
15 Nitawapa nyasi kwenye mashamba yenu kwa ajili ya mifugo yenu, na mtakula
na kushiba. 16 Uwe makini mwenyewe, ili kwamba moyo wako usidanganyike, na
kugeuka na kuabudu miungu mingine, na kuisujudia; 17 ili kwamba hasira ya Yahwe
isiwashiwe dhidi yenu, na ili kwamba asifunge mbingu, kwamba pasiwe na mvua,
na nchi haitavuna matunda, na ili kwamba mpotee kwa haraka kutoka nchi nzuri
ambayo Yahwe anawapa. 18 Kwa hiyo yaweke haya maneno ndani ya moyo wako na
roho; yafunge kama ishara kwenye mkono wako, na yawe utepe katikati ya macho
yako. 19 Utayafundisha kwa watoto na kuongea juu yake wakati uketipo ndani ya
nyumba yako, wakati utembeapo barabarani, wakati ulalapo, na wakati uinukapo.
20 Utayaandika kwenye miimo ya milango ya nyumba zenu na kwenye malango
yenu, 21 kwamba siku zenu na siku za watoto wenu ziweze kuongezeka katika nchi
ambayo Yahwe aliapa kwa mababu zenu kuwapa, maadamu mbingu ziko juu ya
ardhi. 22 Kama mtayashika kwa bidii maagizo haya yote ambayo ninawaamuru

nyinyi, ili kwamba myafanye, mpende Yahwe Mungu wenu, tembea katika njia
zake zote, na kushikamana naye, 23 basi Yahwe atawaondosha mataifa haya yote
kutoka mbele yenu, na mtayafukuza mataifa makubwa na yenye nguvu kuliko nyie.
24 Kila eneo ambalo unyao wa miguu utatembea litakuwa lenu; kutoka jangwani
hadi Lebanoni, toka mto wa Euphratesi, hadi magharibi mwa bahari itakuwa mpaka
wenu. 25 Hakuna mtu ataweza kusimama mbele yenu; Yahwe Mungu wenu ataweka
hofu yenu na ugaidi wenu juu ya nchi yote mnayotembea juu yake kama alivyosema
na ninyi. 26 Tazama, naweka mbele yenu baraka na laana; 27 baraka, kama mtasikiliza
amri za Yahwe ambazo ninakuamuru leo, 28 na laana, kama hamtasikiliza amri
za Yahwe Mungu wenu, lakini mkaicha njia ninayokuamuru leo, kuendea miungu
mingine ambayo hamjaijua. 29 Itakuwa wakati Yahwe Mungu wenu anawaleta ninyi
katika nchi ambayo mnaenda kumiliki, kwamba mtaweka baraka juu ya mlima
Gerizimu na laana juu ya mlima Ebali. 30 Hawako ng'ambo ya pili zaidi ya Yordani,
magharibi mwa barabara la magharibi, katika nchi ya Wakanani wanaoishi Arabah,
juu dhidi ya Gilgali, kando ya mialo ya Moreh? 31 Kwa maana mtavuka ng'ambo
ya pili ya Yordani kuingia kumiliki nchi ambayo Yahwe Mungu wenu anawapa, na
mtamiliki na kuishi ndani yake. 32 Mtashika sheria zote na amri ninazoweka mbele
yenu leo.

# 12

1 Hizi ni amri na sheria ambazo mtazishika katika nchi ambayo, Yahwe Mungu
wa baba zenu, amewapa kumiliki, siku zote mnazoishi kwenye ardhi. 2 Hakika
mtaharibu maeneo yote ambapo mataifa mtakayofukuza miungu yao walioabudu,
kwenye milima mirefu, kwenye vilima, na chini ya kila mti wa kijani. 3 Na
mtazivunja madhabahu zao chini, mtaharibu kwa vipandepande nguzo zao za mawe,
na kuchoma ncha za Asherahi, mtazikata sanaa za kuchongwa za miungu yao na
kuangamiza jina lao nje ya eneo hilo. 4 Hamtamwabudu Yahwe Mungu wenu kama
hivyo. 5 Lakini kwa eneo ambalo Yahwe Mungu wenu atachagua kutoka makabila
yenu kuweka jina lake, hapo patakuwa ni eneo analoishi na huko ndiyo mtaenda.
6 Ni huko ndiko mtaleta sadaka ya kutekeketezwa, dhabihu zenu, zaka zenu, na
sadaka zinazotolewa kwa mkono wenu, sadaka zenu za viapo, sadaka za utayari
na mzao wa kwanza wa mifugo na wanyama. 7 Ni huko mtakula mbele za Yahwe
Mungu wenu na kufurahi kuhusu kila kitu ambacho mmeweka mkono, nyie na jamaa
zenu, ambapo Yahwe Mungu wenu amewabariki. 8 Hamtafanya mambo yote ambayo
tunafanya hapa leo; sasa kila moja anafanya chochote kile kizuri machoni pake,
9 kwa kuwa bado hamjapumzika, kwa urithi ambao Yahwe Mungu wenu anawapa.
10 Lakini pindi mnaenda ng'ambo ya pili ya Yordani na kuishi ndani ya nchi ambayo
Yahwe Mungu wenu anasababisha ninyi kurithi, na wakati awapa pumziko kutoka
kwa maadui zenu wanaowazunga karibu, ili kusudi muishi kwa usalama, 11 kisha
itakuwa eneo ambalo Yahwe Mungu wenu atachagua kusababisha jina lake kuishi,
huko mtaleta yote ninayowaamuru; sadaka za kuteketezwa, dhabihu zenu, zaka
zenu, sadaka zilizotolewa kwa mkono wenu, na sadaka za chaguo lenu kwa ajili
ya nadhiri mtakazotoa kwa Yahwe. 12 Mtafurahi mbele za Yahwe Mungu wenu-
nyie, watoto wenu, binti zenu, wajakazi wa kiume, wajakazi wa kike, na Walawi
walio ndani ya lango lenu, kwa sababu hana sehemu au urithi miongoni mwenu.
13 Uwe makini mwenyewe kwamba usitoe sadaka zako za kuteketezwa kila eneo
unaloona; 14 lakini ni katika eneo hilo ambalo Yahwe atawachagua miongoni moja
kati ya makabila yenu ambalo litatoa sadaka ya kuteketezwa, na huko mtafanya kila
kitu ninachokuamuru. 15 Hata hivyo, mtaweza kuua na kula wanyama ndani ya
malango yenu, kama mnavyotaka, kupokea baraka ya Yahwe Mungu wenu kwa ajili

ya yote amewapa; na watu wasio safi na safi wote wanaweza kula, wanyama kama
vile paa na kulungu. 16 Lakini hamtakula damu, mtaimwaga kwenye ardhi kama
maji. 17 Mnaweza msile ndani ya malango kutoka kwenye zaka ya nafaka zenu,
mvinyo wenu mpya, mafuta yenu au mzao wa kwanza wa mifugo au wanyama; na
mnaweza msile nyama yoyote mnayoitoa dhabihu pamoja na viapo vyovyote vyenu
mnafanya, wala sadaka yenu ya utayari, wala sadaka mnayotoa kwa mkono wenu.
18 Badala yake, mtakula mbele ya Yahwe Mugu wenu katika eneo ambalo Yahwe
Mungu atachagua- nyie, mtoto wenu, binti yenu, mjakazi wa kiume, mjakazi wa kike,
na Mlawi aliye malangoni mwenu; mtafurahi mbele ya Yahwe Mungu wenu kuhusu
kila kitu ambacho mnaweka mkono wenu. 19 Muwe makini wenyewe ili kwamba
msimwache Mlawi maadamu mnaishi kwenye nchi yenu. 20 Wakati Yahwe Mungu
wenu apanua mipaka yenu, kama alivyowaahidi, na kusema, "Nitakula nyama," kwa
sababu ya tamaa zenu mnakula nyama, mnaweza kula nyama, kama tanmaa za
roho zenu. 21 Kama eneo ambalo Yahwe Mungu wenu achagua kuliweka jina lake ni
mbali kutoka kwenu, basi mtaua baadhi ya mifugo yenu na wanyama wenu ambao
Yahwe amewapa, kama nilivyowaamuru: hivyo mnaweza kula ndani ya malango
yenu, kama tamaa za roho zenu. 22 Kama paa na Kulungu wanaliwa, hivyo mtakula
watu wasio safi na wasafi wanaweze kula kadhalika. 23 Lakini muwe na uhakika
kwamba hamtumii damu, kwa kuwa damu ni uhai, hamtakula uhai pamoja na
nyama. 24 Hamtakula, mtaimwaga nje kwenye ardhi kama maji. 25 Hamtakula, ili
kwamba iweze kuwa vizur kwenu, na watoto wenu baada yenu, wakati mtafanya
kile kilicho sahihi machoni pa Yahwe. 26 Lakini mambo ambayo ni ya Yahwe
ambayo mnayo na sadaka za viapo vyenu-mtachukua hizi na kwenda eneo ambalo
Yahwe achagua. 27 Hapo mtatoa sadaka ya kuteketekezwa, nyama na damu, kwenye
madhabahu ya Yahwe Mungu wenu, damu ya dhabihu zenu itamwangwa nje kwenye
madhabahu ya Yahwe Mungu wenu, na mtakula nyama. 28 Mchunguze na msikilize
haya maneno yote ambayo - ninawaamuru, ili iwe uzuri kwenu na watoto wenu
baada yenu milele, wakati mnafanya kile kilicho kizuri na sawa machoni pa Yahwe
Mungu wenu. 29 Wakati Yahwe Mungu wenu anapunguza mataifa kutoka kwenu,
wakati mnaingia kuwafukuza, na mnawafukuza na kuishi katika nchi yao, 30 muwe
makini wenyewe ili kwamba msinaswe kwa kuwafuata, baada ya kuangamizwa
kutoka kwenu kunaswa katika kuchunguza miungu yao, katika kuuliza, "Kwa namna
gani haya mataifa yanaabudu muingu yao? Nitafanya hivyo hivyo. 31 Hautafanya
hivyo katika kumheshimu Yahwe Mungu wako, kwa kuwa kila kitu ambacho ni
chukizo kwa Yahwe, mambo ambayo anayachukia- wamefanya haya na miungu yao,
hata mnateketeza vijana wao na binti zao kwenye moto kwa ajili ya miungu yao.
32 Chochote ninakuamuru, chunguza. Usiongeze juu yake au kupunguza.

# 13

1 Kama miongoni mwenu ainuka nabii au muota ndoto, 2 na kama anawapa ishara
au maajabu, na kama ishara au maajabu yanatokea, kama alivyozungumza kwenu na
kusema, " Ebu tuifuate miungu mingine, ambayo hatuijui, na tuiabudu. 3 Usisikilize
maneno ya nabii huyo, au kwa huyo muota ndoto, kwa kuwa Yahwe Mungu wako
anakujaribu kujua kama unampenda Yahwe Mungu wako kwa moyo wako wote na
roho yako yote. 4 Mtatembea baada ya Yahwe Mungu wenu, mheshimu, mzishike
amri zake, na mtii sauti yake, na mtamwabudu na kushikamana naye. 5 Nabii huyo
au muota ndoto atauwawa, kwa sababu amezungumza uasi dhidi ya Yahwe Mungu
wenu, ambaye aliwaleta toka nchi ya Misri, na aliyewakomboa kutoka nyumba ya
utumwa. Hivyo nabii anataka kuwaondoa katika njia ambayo Yahwe Mungu wenu
aliwaamuru kutembea. Kwa hiyo weka mbali maouvu kutoka kwenu. 6 Tuseme

kwamba ndugu yako, mwana wa mama yako, au mwana wako, au binti yako, au
mke wa karibu nawe, au rafiki yako ambaye ni kama roho yako, kukushawishi kwa
siri na kusema, “Acha tuende na tukaabudu miungu mingine ambayo hatujazijua,
wala wewe wala mababu zako- 7 Miungu yeyote ya watu ambayo imewazunguka,
karibu nanyi au mbali kutoka, kutoka mwisho wa dunia kwenda mwisho mwingine
wa dunia. 8 Usimkubali au kumsikiliza. Wala macho yako yasione huruma, wala
hautamuacha akiba au kumficha. 9 Badala yake, utamuacha hakika; mkono wako
utakuwa wa kwanza kumuua, na badae mkono wa watu wote. 10 Mtamponda
mpaka kufa kwa mawe, kwa sababu amejaribu kuwaondoa kutoka kwa Yahwe
Mungu wenu, ambaye aliwatoa kutoka nchi ya Misri, nje ya nyumba ya utumwa.
11 Israel yote itasikia na kuogopa, na haitaendelea kufanya aina ya uovu miongoni
mwenu. 12 Kama utasikia yeyote anasema kuhusu moja ya miji yenu, kwamba
Yahwe Mungu wenu anawapa kuishi ndani yake. 13 Baadhi ya wenzuni waovu
wamewaacha miongoni mwenu na kuacha kwa mbali wakazi wa miji yao na kusema,
“Acha tuende na kuabudu miungu mingine ambayo hamjaijua. 14 Basi utaichunguza
uthibitisho, kufanya utafiti na kuipeleleza kwa kina. Wakati unagundua kwamba ni
kweli na hakuna shaka kwamba chukizo hilo lililofanyika miongoni mwenu, kisha
utachukua hatua. 15 Utawashambulia hakika wenyeji wa mji huo kwa makali ya
upanga. Utaangamiza kabisa na watu wote walio ndani yake, pamoja na mifugo yake,
pamoja na makali ya upanga. 16 Utakusanya nyara zote kutoka katikati mwa mitaa
yake na utuunguza mji, pamoja na nyara zake zote - kwa kuwa Yahwe Mungu wako.
Mji utakuwa mchungu wa uharibifu milele; haupaswi kujengwa tena. 17 Hakuna hata
kimoja kati ya vitu hivyo vimewekwa wakfu kwa ajili ya kuangamizwa vinapaswa
kugadamana kwenye mkono wako. Hii inapaswa kuwa kesi, ili kwamba Yahwe
atageuka kutoka kwenye ukali wa hasira yake, kumuonyesha rehema, kuwa na
huruma kwako, na kukufanya wewe kuogezeka katika idadi, kama alivyoapa kwa
baba zako. 18 Atafanya hivi kwa sababu unasikiliza sauti ya Yahwe Mungu wako,
kuzishika amri zake ambazo ninakuamuru leo, kufanya kile kilicho sahihi mbele ya
macho ya Yahwe Mungu wako.

# 14

1 Ninyi ni watu wa Yahwe Mungu wenu. Msijikate wenyewe, wala kunyoa sehemu
za nyuso zenu kwa ajili ya wafu. 2 Kwa kuwa mu taifa lilowekwa wakfu kwa Yahwe
Mungu wenu, na Yahwe amewachagua kuwa watu kwa ajili ya urithi wake, zaidi
kuliko watu wote walio juu ya uso wa dunia. 3 Hampaswi kula kitu chochote kilicho
chukizo. 4 Hawa ni wanyama ambao mnaweza kula: ng'ombe, kondoo, mbuzi,
5 kulungu, paa, kulungu wa kiume, mbuzi wa mwituni, paa mweupe na pofu na
kondoo wa mlimani 6 Mnaweza kula wanyama wowote ambao wamegawanyika
kwato, ambaye ana kwato zilizogawanyika mara mbili, na utafuna macheuo. 7 Hata
hivyo, hampaswi kula baadhi ya wanyama ambao utafuna macheuo au ambao
wana kwato zilizogawanyika mara mbili: ngamia, sungura, pomono, kwa sababu
watafuna macheuo lakini hawajagawanyika kwato, ni najisi kwenu. 8 Nguruwe ni
najisi kwenu pia kwa sababu amegawanyika kwato lakini hatafuni macheuo; ni
najisi kwenu. Msile nyama ya nguruwe, na msiguse mizoga yao. 9 Haya yaliyo
ndani ya maji mnaweza kula: chochote kilicho na mapesi na magamba; 10 lakini
chochote kisichokuwa na mapesi na magamba msile; ni najisi kwenu. 11 Ndege wote
safi mnaweza kula. 12 Lakini hawa ni ndege ambao hampaswi kula: tai, tumbusi,
kipungu, 13 mwewe mwekundu na mweusi, aina yoyote ya kipanga. 14 Hampaswi
kula aina yoyote ya kunguru, 15 na mbuzi na mwewe wa usiku, Lanes ndege wa
baharini, aina yoyote ya mwewe, 16 bundi mdogo, bundi mkubwa, na bundi mweupe,

[17] Mwari, nyamafu ya tai, mnandio. [18] Hampaswi kula korongo, aina yoyote ya
kongoti, hudihudi, na popo. [19] Wote wenye mabawa; vitu vya utando ni najisi
kwenu; havipaswi kuliwa. [20] Mnaweza kula vitu vyote virukavyo. [21] Hampaswi
kula chochote kinachokufa chenyewe; mnaweza kumpa mgeni ambaye yuko katika
mji wenu, kwamba anaweza kula au mnaweza kuuza kwa mgeni. Kwa kuwa mu
taifa lilolowekwa wakfu kwa ajili ya Yahwe Mungu wenu. Hampaswi kumchemusha
mbuzi kijana katika maziwa ya mama yake. [22] Hakika mnapaswa kutoa fungu la
kumi la mavuno ya mbegu zenu zote, ambazo huja kutoka kwenye shamba kila
mwaka. [23] Mnapaswa kula mbele ya Yahwe Mungu wenu, katika eneo ambalo
atachagua kama patakatifu pake, fungu la kumi la nafaka zenu, za mvinyo mpya,
na mafuta yenu, na mzaliwa wa kwanza wa wanyama na mifugo, kwamba mnaweza
kujifunza daima kumheshimu Yahwe Mungu wenu. [24] Kama safari ni ndefu kwenu na
kwamba hamwezi kuibeba, kwa sababu eneo ambalo Yahwe Mungu wenu atachagua
kama patakatifu pake ni mbali kwenu, basi, wakati Yahwe Mngu anawabariki,
[25] mtabadilisha sadaka katika pesa. Fungeni pesa kwenye mkono, na nendeni kwenye
eneo ambalo Yahwe Mungu wenu atachagua. [26] Huko mtatumia pesa kwa chochote
mnatamani kwa ng'ombe au kondoo, au kwa mvinyo, au kwa kinywaji imara, au kwa
chochote mnatamani; mtakula hapo mbele ya Yahwe Mungu wenu, na mtafurahi,
nyie na nyumba zenu. [27] Mlawi ambaye yuko malangoni mwenu- msimsahau, kwa
kuwa hana sehemu wala urithi pamoja nanyi. [28] Mwisho mwa kila miaka mitatu
mtawasilisha mafungu yote ya kumi ya mazao kwa mwaka huo huo, na mtatunza
katika malango yenu; [29] na Mlawi, kwa sababu hana sehemu wala urithi pamoja
nanyi, na mgeni, na yatima, na wajane walio ndani ya malango yenu, watakuja na
kula na kurithika. Fanya hivyo kwa Yahwe Mungu wenu aweze kuwabariki katika
kazi zote za mikono yenuo mnazofanya.

# 15

[1] Kila mwisho wa kila miaka saba, mnapaswa kufuta madeni. [2] Hii ni tabia ya
ukombozi. Kila mkopeshaji atafuta kile alichompa jirani yake, hata dai kutoka kwa
jirani yake au ndugu yake kwa sababu ufutaji wa madeni wa Yahwe umetangazwa.
[3] Kutoka kwa mgeni mnaweza kudai; lakini kwa chochote chenu kilicho na ndugu
yenu mnapaswa mkitoe. [4] Hata hivyo, pasiwepo maskini miongoni mwenu (kwa
kuwa Yahwe kwa hakika atawabariki kwenye nchi ambayo anawapa kama urithi
kumiliki) [5] kama peke yenu mnasikiliza kwa bidii sauti ya Yahwe Mungu wenu,
kuzishika amri zote ambazo anawaamuru leo. [6] Kwa kuwa Yahwe Mungu wenu
atawabariki, kama alivyowaahidia; mtakopesha mataifa mengi, lakini hamtaazima;
mtaongoza juu ya mataifa mengi, lakini hayatawaongoza ninyi. [7] Kama kuna mtu
maskini miongoni mwenu, moja wa ndugu zenu, ndani ya malango yenu yoyote
kwenye nchi yenu ambayo Yahwe Mungu wenu anawapa, msifanye migumu mioyo
yenu wala kufunga mkono wenu toka kwa ndugu yenu, [8] Lakini mnapaswa hakika
kufungua mkono wenu kwake na hakika mkopeshe yeye vya kutosha hitaji lake.
[9] Muwe makini kutokuwa na wazo ovu au potovu katika moyo wenu, kusema,
“Mwaka wa saba, mwaka wa ukombozi u karibu; ili kwamba msiwe wachoyo
kuhusiana na ndugu zenu maskini na haumpi chochote; anaweza kumlilia Yahwe
kuhusu nyie, na itakuwa dhambi yenu. [10] Mnapaswa kwa hakika mmpe, na moyo
wenu hampaswi kuhuzunika wakati mnampa, kwa sababu kurudishiwa kwa Yahwe
huyu Mungu wenu atawabariki katika kazi zenu zote na katika chochote mnaweka
mkono wenu. [11] Kwa kuwa maskini kamwe hatakoma kuishi katika nchi, kwa hiyo
nakuamuru wewe na kusema, “Unapaswa kwa hakika ufungue mkono wako kwa
ndugu yako, kwa mhitaji wako, na kwa maskini wako katika nchi yako. [12] Kama

ndugu yako, ni mwebrania wa kiume au mwebrania wa kike, ameuzwa kwako na
anakutumikia kwa miaka saba, basi katika mwaka wa saba unapaswa umwache
aende zake huru. 13 Unapomwacha aende zake huru, usimwache aende mkono
mtupu. 14 Unapaswa kwa ukarimu hutoe kwake kutoka mifugo yako, kutoka pura
iliyo chini, na kinu chako cha mvinyo. Kama Yahwe Mungu wako alivyokubariki,
unapaswa umpe yeye. 15 Unapaswa kukumbuka kwamba ulikuwa mtumwa kwenye
nchi ya Misri, na kwamba Yahwe Mungu wako alikukomboa; kwa hiyo ninakuamuru
leo kufanya hivi. 16 Itakuwa kwamba kama atasema kwako, "Sitaenda mbali
yako; kwa sababu anakupenda na nyumba yako, na kwa sababu ni mzuri kwako,
17 basi unapaswa kuchukua uma na msukumo kupitia sikio lake kwenye mlango,
na atakuwa mtumwa wako milele. Na pia kwa mtumwa wako wa kike utafanya
vilevile. 18 Isionekane kuwa vigumu kwako kumwachia aende zake huru, kwa
sababu amekutumikia kwa miaka sita na amekupa mara mbili udhamani wa mtu
aliyeajiriwa. Yahwe Mungu wako atakubariki katika yote unayofanya. 19 Wazao wote
wa kwanza wa kiume katika wanyama na mifugo wako unapaswa uwatenge kwa
Yahwe Mungu wako. Hautafanya kazi na mzao wa kwanza wa wanyama wako wala
kumnyoa mzao wa kwanza wa mfugo wako. 20 Unapaswa umle mzaliwa wa kwanza
mbele ya Yahwe Mungu wako kila mwaka katika eneo ambalo Yahwe atachagua,
wewe na nyumba yako. 21 Kama ina kasoro yoyote- kwa mfano, kama ni kilema
au kipofu, au ana kasoro yoyote- haupaswi kumtoa dhabihu kwa Yahwe Mungu
wako. 22 Utamla ndani ya malango yako; mtu asiye najisi na aliye najisi ni sawa
unapaswa kula, kama ungekula paa au kulungu. 23 Pekee haupaswi kunywa damu
yake; unapaswa kuimwanga damu yake juu ya ardhi kama maji.

# 16

1 Angalia mwezi wa Abibu, na uishike pasaka ya Yahwe Mungu wako, kwa kuwa
katika mwezi wa Abibu Yahwe Mungu wako alikuleta toka Misri usiku. 2 Utamtolea
dhabibu ya pasaka Yahwe Mungu wako na baadhi ya mifugo na wanyama kwenye
eneo ambalo Yahwe atachagua kama patakatifu pake. 3 Hautakula mkate wa chachu
pamoja nayo, siku saba utakula mkate usio na chachu, mkate wa mateso; kwa kuwa
mlitoka katika nchi ya Misri kwa haraka. Fanya haya katika siku zako zote za
maisha yako ili uweze kukumbuka akilini siku mliotoka nchi ya Misri. 4 Hakuna
chachu inapaswa kuonekana miongoni mwenu ndani ya mipaka yenu wakati wa
siku saba; wala nyama yoyote mnayotoa dhabihu jioni kwa siku ya kwanza inabaki
mpaka asubuhi. 5 Msitoe dhabihu ya pasaka kati ya malango yenu ya ndani ambayo
Yahwe Mungu wenu anawapa. 6 Badala yake, toa dhabihu katika eneo ambalo Yahwe
Mungu wenu atachagua kama patakatifu pake. Hapo mtatoa dhabihu ya pasaka jioni
wakati jua linazama, kwa wakati huo wa mwaka mlitoka Misri. 7 Mtapaswa kuichoma
na kuila katika eneo ambalo Yahwe Mungu wenu atachagua; asubuhi mtageuka na
kwenda kwenye mahema yenu. 8 Kwa siku sita mtakula mkate usiotia chachu; katika
siku ya saba kutakuwa na kusanyiko makini kwa ajili ya Yahwe Mungu wenu; katika
siku hiyo hamtafanya kazi. 9 Mtahesabu wiki saba kwa ajili yenu; tangu wakati
mlipoanza kuweka mundu kwenye nafaka iliyosimama mtapaswa kuanza kuhesabu
wiki saba. 10 Mtapaswa kushika wiki za sherehe ya Yahwe Mungu wenu pamoja
na mchango wa sadaka ya utayari kutoka mkono wako ambayo utatoa, kulingana
na Yahwe alivyokubariki. 11 Utafurahi mbele ya Yahwe Mungu wako- wewe, kijana
wako, binti wako, mjakazi wako wa kiume, mjakazi wako wa kike, Mlawi aliye
katika malango yako, na mgeni, yatima, na mjane alio miongoni mwenu, katika eneo
ambalo Yahwe Mungu wako atachagua kwa ajili ya patakatifu pake. 12 Utakumbuka
akilini kwamba ulikuwa mtumwa Misri; unapaswa kuangalia na kuzishika amri hizi.

[13] Unapaswa kushika sherehe za vibanda kwa siku saba baada ya kuwa mmekusanya
mavuno toka kwenye sakafu ya mapura na kutoka kwenye kinu chako cha divai.
[14] Utafurahi wakati wa sherehe- wewe, kijana wako, binti wako, mjakazi wako
wa kiume, mjakazi wako wa kike, Mlawi, na mgeni, na yatima na mjane walio
ndani ya malango yako. [15] Kwa siku saba unapaswa kuangalia sherehe ya Yahwe
Mungu wako katika eneo ambalo Yahwe atachagua, kwa sababu Yahwe Mungu wako
atakubariki katika mavuno yako yote na kazi ya mikono yako yote, na unapaswa
kuwa na furaha kabisa. [16] Mara tatu kwa mwaka wanaume wako wote wanapaswa
kuonekana mbele za Yahwe Mungu wako katika eneo ambalo atachagua: katika
sherehe ya mkate usiotiwa chachu, katika sherehe za wiki, na sherehe ya vibanda;
na hawataonekana mbele za Yahwe mikono mitupu; [17] badala yake, kila mtu atatoa
kama awezavyo, kwamba mtajua baraka kwamba Yahwe Mungu wako amekupa.
[18] Unapaswa kufanya waamuzi na maakida ndani ya malango yako ambayo Yahwe
Mungu wako anakupa; watachukuliwa toka kila kabila, and watahukumu watu
kwa hukumu ya haki. [19] Haupaswi kuiondoa haki kwa nguvu; haupaswi kuonesha
upendeleo wala kuchukua rushwa, kwa kuwa rushwa upofusha macho ya hekima
na kupotosha maneno ya haki. [20] Unapaswa kufata baada ya haki, baada ya haki
peke yake, ili kwamba uishi na kurithi nchi ambayo Yahwe Mungu wako anakupa.
[21] Haupaswi kujitengenezea Asherahi, aina yoyote ya mti, kando ya madhabahu
ya Yahwe Mungu wako ambayo utakayojitengenezea. [22] Wala usijitengenezee jiwe
takatifu la nguzo, ambalo Yahwe Mungu wako anachukia.

# 17

[1] Haupaswi kumtolea dhabihu Yahwe Mungu wako ng'ombe au kondoo aliye na
kasoro au kitu chochote kibaya, kwa kuwa hiyo itakuwa chukizo kwa Yahwe Mungu
wako. [2] Kama kunapatikana miongoni mwenu, ndani ya malango ya mji wowote
ambao Yahwe Mungu wenu anawapatia, mwanaume yoyote au mwanamke ambaye
anafanya uovu mbele ya Yahwe Mungu wenu kuiharibu agano lake - [3] yoyote ambaye
ameenda na kuabudu miungu mingine na kuisujudia, wala jua, mwezi, au kati ya
jeshi la mbinguni- hakuna chochote nimekuamuru, [4] na kama ungeambiwa kuhusu
hiki, au kama una mifugo- basi unapaswa kufanya uchunguzi wa makini. Kama ni
kweli na hakika kwamba chukizo kama hilo limefanyika Israeli- [5] -basi utamleta huyo
mwanaume au mwanamke, aliyefanya uovu huu, katika malango ya mji, kwamba
mwanaume kabisa au mwanamke, na umponde huyo mtu mpaka kufa. [6] Kwa
kinywa cha mashahidi wawili, au mashahidi watatu, itakuwa yeye anayepaswa
kuuwawa; lakini kwa kinywa cha shahidi mmoja peke hatauwawa. [7] Mkono wa
mashahidi unapaswa kuwa wa kwanza kumuuwa, na badae mkono wa watu wote;
na mtamuondoa muovu miongoni mwenu. [8] Kama jambo linatokea ambalo ni gumu
kwenu kufanya maamuzi- pengine swali la mauaji au kifo cha ajali, haki ya mtu
mmoja na haki ya mtu mwingine, au swali moja la aina ya kuzulu kufanyika, au
aina nyingine ya jambo-mambo ya utata ndani ya malango yenu, basi utapaswa
kwenda kwenye eneo ambalo Yahwe Mungu wako atachagua kama patakatifu pake.
[9] Utapaswa kwenda kwa makuhani, wazao wa Lawi, na kwa mwamuzi atakayetumika
kwa wakati huo; mtatafuta ushauri wao, na watawapa ninyi maamuzi. [10] Mnapaswa
kufuata sheria mliyopewa, katika eneo Yahwe atachagua kama patakatifu pake.
Mtakuwa makini kufanya kila kitu ambacho wanawaelekeza kufanya. [11] Fuata
sheria wanayowafundisha, na kufanya kulingana na maamuzi wanawapa. Msigeuke
kutoka kwa kile wanawambia, kwa kulia au kushoto. [12] Yeyote anayefanya kwa
kiburi, kwa kutomsikiliza kuhani anayesimama kutumika mbele ya Yahwe Mungu
wako, au kwa kutomsikiliza mwamuzi- huyu mtu atakufa; mtaweka mbali uovu

kutoka Israeli. [13] Watu wote wanapaswa kusikia na kuogopa, na kutofanya kwa
kiburi tena. [14] Wakati mlipokuja kwenye nchi ambayo Yahwe Mungu anawapa, na
wakati mnamiliki na kuanza kuishi ndani yake, na halafu unasema, 'Nitajiwekea
mfalme juu yangu, kama mataifa yote yanayonizunguka mimi,' [15] basi unapaswa kwa
hakika kujiwekea mfalme juu yako mtu yeyote ambaye Yahwe atachagua. Unapaswa
kujiweka kama mfalme juu yako mtu yeyote kutoka miongoni mwa ndugu zenu.
Haupaswi kuweka mgeni, ambaye si ndugu yenu, juu yenu. [16] Lakini hapaswi
kuzidisha farasi kwa ajili yake, wala kusababisha watu kurudi Misri ili kwamba
aweze kuzidisha farasi, kwa kuwa Yahwe alikwisha sema kwako, 'Unapaswa kuanzia
sasa usirudi njia hiyo tena.' [17] Na hapaswi kuzidisha wake kwa ajili yake, ili kwamba
moyo wake usigeuke kotoka kwa Yahwe; wala hapaswi sana kuzidisha kwa ajili
yake fedha au dhahabu. [18] Wakati aketipo kwenye kiti cha enzi cha ufalme wake,
anapaswa kuandika kwenye kitabu kwa ajili yake nakala ya sheria hii, kutoka kwenye
sheria ambayo iko mbele ya makuhani, ambao ni Walawi. [19] Kitabu kinapaswa
kuwa na yeye, na anapaswa kusoma ndani yake kwa siku zake zote, ili kwamba
aweze kujifunza kumheshimu Yahwe Mungu wako, ili kwamba ashike maneno yote
ya sheria hii na amri hizi, kuzishika. [20] Anapaswa kufanya hivi ili kwamba moyo
wake usiinuliwe zaidi ya ndugu zake, na ili kwamba asigeuke mbali na amri, kwa
kulia au kwa kushoto' kwa kusudi kwamba aweze kuzidisha siku zake katika ufalme
wake, yeye na watoto wake, miongoni mwa Israel.

# 18

[1] Makuhani, ambao ni Walawi, na makabila yote ya Lawi, hayatakuwa na mgao
wala urithi pamoja na Israel; wanapaswa kula dhabihu ya Yahwe iliyotengenezwa
kwa moto kama urithi wao. [2] Hawatakuwa na urithi miongoni mwa ndugu zao;
Yahwe ni urithi wao, kama alivyosema nao. [3] Hii ni sababu ya makuhani kutoka
kwa watu, kutoka kwa wale wanaotoa dhabihu, kama itakuwa ng'ombe au kondoo:
wanapaswa kutoa kwa kuhani bega, mashavu mawili, na sehemu za ndani. [4] Mazao
ya kwanza ya nafaka zako, mvinyo wako mpya, na mafuta yako, na manyoya
ya kwanza ya kondoo zako, unapaswa umpe. [5] Kwa kuwa Yahwe Mungu wako
amemchagua kutoka kwenye makabila yote yako kusimama kutumika kwa jina la
Yahwe, yeye na wana wake milele. [6] Kama Mlawi anatoka kati ya miji yenu nje ya
Israel yote kutoka ambapo anaishi, na utamani kwa moyo wake wote kuja katika eneo
Yahwe atachagua, [7] basi anapaswa kutumika kwa jina la Yahwe Mungu wake kama
ndugu zake wote Walawi wanafanya, wanaosimama mbele ya Yahwe. [8] Wanapaswa
kuwa na mgao wa kufanana wa kula, badala ya kile kinachokuja kutokana na mauzo
ya urithi wa familia yake. [9] Wakati mmekuja katika nchi ambayo Yahwe Mungu wenu
anawapa, mnapaswa kujifunza kuangalia machukizo ya mataifa. [10] Pasipatikana
miongoni mwenu mmoja anayemweka kijana wake au binti yake kwenye moto,
yeyote anatumia uganga, yeyote anatabiri, au mchawi, mchawi yeyote, [11] yeyote
aongeae na wafu, au yeyote aongeae na roho. [12] Kwa yeyote afanyae mambo haya ni
chukizo kwa Yahwe; ni kwa sababu ya machukizo haya ambayo Yahwe Mungu wenu
anawaondosha mbele zenu. [13] Mnapaswa kuwa wakamilifu mbele ya Yahwe Mungu
wenu. [14] Kwa mataifa haya ambayo mtayafukuza kusikiliza wale wafanyao uchawi
na uganga; lakini kwenu, Yahwe Mungu wenu amewakataza ninyi kufanya hivyo.
[15] Yahwe Mungu wenu atainua kwa ajili yenu nabii kutoka miongoni mwenu, mmoja
wa ndugu zenu, kama mimi. Mnapaswa kumsikiliza. [16] Hiki ndicho mlichouliza
kutoka kwa Yahwe Mungu wenu huko Horebu katika siku ya kusanyiko, kusema,
“Acha tusisikie tena sauti ya Yahwe Mungu wetu, wala kuona moto mkuu tena, wala
tutakufa.” [17] Yahwe alisema nami, “Kile walichosema ni kizuri. [18] Nitamwinua nabii

kwa ajili yao kutoka miongoni mwa ndugu zao, kama wewe. Nitaweka maneno yangu
katika kinywa chake, na ataongea nao yote niliyowakuamuru. 19 Itakuwa kama
yeyote hatasikia maneno yangu ambayo anazungumza kwa jina langu, nitalitaka
kwake. 20 Lakini nabii ambaye anazungumza neno kwa kiburi kwa jina langu,
neno ambalo sijamuamuru kusema, au ambaye anayezungumza kwa jina la miungu
mingine, huyo nabii atakufa. 21 Hivyo ndivyo unapaswa kusema katika mioyo yenu:
“Tutagunduaje kuwa ujumbe ambao Yahwe hajazungumza? 22 Mtagundua ujumbe
ambao Yahwe amezungumza pindi nabii azungumzapo kwa jina la Yahwe. Kama
hiyo haitokei wala kufanyika, basi hicho ni kile ambacho Yahwe hajazungumza na
nabii amezungumza kwa kiburi, na hampaswi kumuogopa.

# 19

1 Wakati Yahwe Mungu wenu anayafutilia mbali mataifa, yale ambayo Yahwe
Mungu wenu anawapa nchi yao, na wakati mnakuja kwao na kuishi katika miji yao
na nyumba, 2 mnapaswa kuchagua miji mitatu kwa ajili yenu katikati mwa nchi yenu
ambayo Yahwe Mungu anawapa kuimiliki. 3 Mnapaswa kujenga barabara na kugawa
mipaka ya nchi yenu katika maeneo matatu, nchi ambayo Yahwe Mungu wenu
anafanya kuimiliki, ili kwamba kila mmoja anayeua mtu mwingine apate kukimbia
hapo. 4 Hii ni sheria kwa ajili ya mtu anayeua mwingine na anayekimbilia huko
kuishi: yeyote auae jirani yake bila kujua, na hapo awali hakumchukia- 5 kama wakati
mtu aingiapo katika msitu pamoja na jirani yake kukata kuni, na mkono wake ukata
mti chini kwa shoka, na kichwa uteleza kutoka kwenye mpini na kumpiga jirani yake
mpaka akafa- basi mtu huyu anapaswa kukimbilia katika moja ya miji hii na kuishi.
6 Vinginevyo damu ya mlipiza kisasi atamfuata yeye aliyetoa uhai, na kwa hasira kali
anampita kwa sababu ilikuwa safari ndefu. Na anampiga na kumuua, ijapokuwa mtu
huyo akustahili kufa; na hata akustahili adhabu ya kifo kwa sababu hakumchukia
jirani yake kabla hili halijatokea. 7 Basi sasa ninakuamuru kuchagua miji mitatu
kwa ajili yako. 8 Kama Yahwe Mungu wenu apanua mipaka yenu, kama alivyoapa
kwa mababu zenu kufanya, na kuwapa nchi yote ambayo amewaahadia kuwapa
mababu zenu; 9 kama mnazishika amri hizi zote kuzifanya, ambazo ninakuamuru
leo- amri za kumpenda Yahwe Mungu wenu na daima kutembea katika njia zake,
basi mnapaswa kuongeza miji mitatu zaidi kwa ajili yenu, isipokuwa ile mitatu.
10 Fanya hivi ili kwamba damu isiyo na hatia isimwangwe katikati ya nchi ambayo
Yahwe Mungu wenu anawapa kwa ajili ya urithi, ili kwamba pasiwepo hatia ya
damu kwenu. 11 Lakini kama yeyote anamchukia jirani yake, uongo unamsubiri,
uinuka dhidi yake, na majeraha ya kufa kwake ili kwamba anakufa, na kama basi
anakimbia katika moja ya miji hii- 12 basi wazee wa mji wake wanapaswa kumtoa na
kumrudisha toka huko, na kumkabizi katika mkono wa ndugu mhusika, ili kwamba
amuue. 13 Jicho lako halipaswi kumuonea huruma; badala yake; unapaswa kuondoa
hatia ya damu kutoka Israel, ili kwamba iwe vizuri kwako. 14 Haupaswi kuondoa
alama ya jirani yako ambayo wameweka katika eneo muda mrefu, katika urithi wako
ambao utarithi, katika nchi ambayo Yahwe Mungu wako anakupa kumiliki. 15 Shahidi
moja peke hapaswi kuinuka dhidi ya mtu kwa ajili ya uovu wowote, au kwa ajili
ya dhambi yoyote, katika jambo lolote ambalo amefanya dhambi; kwa kinywa cha
mashahidi wawili, au kwa kinywa cha mashahidi watatu, kunapaswa jambo lolote
lilithibitishwe. 16 Kama ushuhuda wa mtu asiye na haki anainua dhidi ya mtu yeyote
kushuhudia dhidi yake kwa mambo mabaya. 17 Basi watu wote wawili, mmoja kati
ya yule utata upo, anapaswa kusimama mbele ya Yahwe, mbele ya makuhani na
waamuzi ambao wanatumika siku hizo. 18 Waamuzi wanapaswa kuchunguza kwa
uangalifu; ona, kama ushahidi ni ushahidi wa uongo na umeshuhudiwa kwa uongo

dhidi ya ndugu yake, 19 basi unapaswa kufanya kwake, kama alivyokusudia kufanya
kwa ndugu yake, na utaondoa uovu kutoka miongoni mwenu. 20 Basi wale wanaobaki
watasikia na kuogopa, na kuanzia hapo na kuendelea hawatafanya tena aina ya
ouvu miongoni mwao. 21 Macho yako hapaswi kuona huruma; maisha yatalipa kwa
maisha, jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu.

# 20

1 Pindi utokapo kwenda vitani kupigana dhidi ya adui zako, na kuona farasi,
magari, na watu wengi zaidi kuliko wewe, haupaswi kuwaogopa; kwa kuwa Yahwe
Mungu wako yu pamoja nawe, yeye aliyekuleta kutoka nchi ya Misri. 2 Wakati
unakaribia kuingia kwenye vita, kuhani anapaswa kuwasogelea na kuongea na watu.
3 Anapaswa kuwaambia,"Sikilizeni, Israel, mnaenda kupigana dhidi ya maadui zenu.
Msidhofishe moyo wenu. Msiohofu au kutetemeka. Msiwaogope. 4 Kwa kuwa Yahwe
Mungu wenu ndiye aendae pamoja nanyi kupigana kwa ajili yenu dhidi ya maadui
zenu na kuwaokoa. 5 Maakida wanapaswa kuzungumza na watu na kusema, "Ni mtu
yupi aliyejenga nyumba mpya na hajaiweka wakfu? Acha aende na arudi nyumbani
kwake, ili kwamba asife vitani na mtu mwingine aiweke wakfu. 6 Kuna yeyote
ambaye amepanda mzabibu na hajafurahia matunda yake? Acha aende nyumbani,
ili kwamba asife vitani na mtu mwingine afurahie matunda yake. 7 Ni mtu yupi
aliyeposa kuoa mwanamke lakini bado hajamuoa? Acha aende nyumbani ili kwamba
asife vitani na mume mwingine amuoa." 8 Maakida wanapaswa kuzungumza zaidi
kwa watu na kusema, "Ni mwanaume gani aliye hapa ambaye ni mwenye hofu au
mnyonge? Acha aende na arudi nyumbani kwake, ili kwamba moyo wa ndugu yake
usiyeyuke kama moyo wake. 9 Wakati maakida wamemaliza kuzungumza na watu,
wanapaswa kuteua majemedari juu yao. 10 Wakati mtokapo kuteka mji, wafanye
watu hao toleo la amani. 11 Kama watapokea amani na kufungua malango yao kwako,
watu wote wanaopatikana ndani yake wanapaswa kulazimishwa kukufanyia kazi na
wanapaswa kukutumikia. 12 Lakini kama haitengenezi amani kwenu, lakani badala
yake inatengeneza vita dhidi yenu, basi mnapaswa kumruhusu, 13 na wakati Yahwe
Mungu wenu anawapa ushindi na kuwaweka chini ya utawala wenu, mnapaswa
kuua kila mtu katika mji. 14 Lakini wanawake, wadogo, ng'ombe, na kila kitu kilicho
ndani ya mji, na nyara zake zote, utavichukua kama mateka yako. Nawe utawamaliza
mateka wa maadui zako, ambao Yahwe Mungu amekupa. 15 Unapaswa kuifanyia
hivyo kuelekea miji yote ambayo iko mbali nawe, miji ambayo siyo miji ya mataifa
yafuatayo. 16 Katika miji ya watu hawa ambayo Yahwe Mungu wenu anawapa kama
urithi, mnapaswa kutunza chochote kilicho na uhai. 17 Badala yake, mnapaswa kabisa
kuagamiza: Hittite, na Amorite, Wakanani, Waperezi, Hivite, na Wabusi, kama Yahwe
Mungu wenu alivyowaamuru. 18 Fanya hivi ili kwamba wasiwafundishe kufanya
katika njia za machukizo, kama walivyofanya kwa miungu yao. Kama mtafanya,
mtafanya dhambi dhidi ya Yahwe Mungu wenu. 19 Wakati mtakapouzingira mji kwa
muda mrefu, huku mkipigana dhidi yake kuuteka, hampaswi kuharibu miti yake kwa
kushika shoka dhidi yake. Kwa kuwa utaweza kula matunda yake, kwa hiyo usiikate.
Kwa maana mti wa kondeni mtu ambaye atauzingira? 20 Ila miti ambayo unaijua siyo
miti ya chakula, unaweza kuharibu na kuikata chini; utajenga maburuji dhidi ya mji
unaofanya vita nawe, mpaka uanguke.

# 21

1 Iwapo mtu amekutwa kauwawa ndani ya nchi ambayo Yahwe Mungu wako
anawapatia kumiliki, kalala shambani, na haijulikani aliyemshambulia; 2 basi wazee
wenu pamoja na waamuzi wenu wanapaswa kutoka nje, na kupima katika miji

ambayo inamzunguka yule aliyeuawa. [3] Kisha wazee wa mji ulio karibu na mwili wa
marehemu wanapaswa kuchukua mtamba kutoka kwenye kundi la mifugo, ambaye
hajawahi kutumikishwa, wala kubebeshwa nira. [4] Kisha wanapaswa kumuongoza
mtamba huyo mpaka chini ya bonde litiririkalo maji, bonde ambalo halijawahi
kulimwa wala kupandwa, na mle bondeni wanapaswa kuvunja shingo ya mtamba
huyo. [5] Makuhani, uzao wa Lawi, wanapaswa kuja mbele, kwa maana Yahwe Mungu
wako amewachagua wamtumikie yeye na kutoa baraka katika jina la Yahwe na
kuamua kila mtafaruku na ugomvi kwa neno lao. [6] Wazee wote wa mji ulio karibu na
mtu aliyeuawa wanapaswa kunawa mikono yao juu ya mtamba aliyevunjwa shingo
bondeni; [7] na wanapaswa kutoa suhulisho juu ya jambo hilo na kusema, 'Mikono yetu
haijamwaga damu hii, wala macho yetu hayajaona suala hili. [8] Tusamehe watu wako
Israeli, Yahwe, ambao umewakomboa, na usiweke hatia juu ya umwagaji damu usio
na kosa miongoni mwa watu wako Israeli. ' Kisha umwagaji damu utasamehewa
kwao. [9] Kwa njia hii utaweka mbali umwagaji damu usio na hatia miongoni mwenu,
mtakapofanya yaliyo mema machoni pa YAHWE. [10] Utakapokwenda kupigana vita
dhidi ya maadui zako na Yahwe Mungu wako atakapokupa ushindi na kuwaweka
chini ya mamlaka yako, na ukawachukua mbali kuwa mateka, [11] kama kati ya mateka
ukamwona mwanamke mzuri, nawe ukamtamani na kutaka kujitwalia awe mke
wako, [12] basi utamleta nyumbani kwako; atanyoa nywele zake na kukata kucha zake.
[13] Kisha atazivua nguo alizokuwa amezivaa wakati alipochukuliwa mateka na atabaki
nyumbani kwako na kuwaomboleza baba yake na mama yake kwa mwezi mzima.
Baada ya hapo unaweza kulala naye na kuwa mume wake, naye atakuwa mke wako.
[14] Lakini usipofurahishwa naye, basi unatakiwa kumruhusu aondoke apendaye
yeye. Lakini haupaswi kamwe kumuuza kwa fedha, pia haupaswi kumfanya kama
mtumwa, kwa sababu umemdhalilisha. [15] Iwapo mwanamume ana wake wawili na
mmoja wao ampenda na mwingine kumchukia, na wote wamekwisha mzalia watoto
–wote mwanamke mpendwa na mwanamke achukiwae – [16] basi katika siku ambayo
mwanamume atakapowarithisha mali zake wanawe, hapaswi kumfanya mwana wa
mke ampendaye kuwa mzawa wa kwanza kabla ya mwana wa mke amchukiaye,
ambaye ndiye mwana wa kwanza. [17] Badala yake, anapaswa kumtambua mwana
wa kwanza, mwana wa mke asiyempenda, kwa kumpatia mara mbili ya mali zake;
kwa maana huyo mwana ni mwanzo wa nguvu zake; haki za mzawa wa kwanza ni
zake. [18] Iwapo mwanamume ana mwana mkaidi na muasi ambaye hatatii sauti ya
baba yake au sauti ya mama yake, ambaye, hata baada ya kurekebishwa, hatawasikia;
[19] basi baba yake na mama yake wanapaswa kumshika na kumleta mbele ya wazee
wa mji na kwenye malango ya mji. [20] Wanapaswa kuwaambia wazee wa mji, "Huyu
mwanetu ni mkaidi na muasi; hataki kusikia sauti zetu; ni mwasherati na pia ni
mlevi'. [21] Kisha wanaume wote wa mji wanapaswa kumpiga kwa mawe hadi kufa;
nanyi mtaondoa uovu miongoni mwenu. Israeli yote itasikia juu ya hili na kuogopa.
[22] Iwapo mwanamume kafanya dhambi inayostahili kifo na kisha akauwawa, kwa
kunyongwa juu ya mti, [23] basi mwili wake haupaswi kubaki usiku kucha juu ya
mti. Badala yake, unapaswa kuhakikisha unamzika siku hiyo; kwa maana yeyote
anyongwaye amekwisha laaniwa na Mungu. Tii amri hii ili kwamba usitie najisi
nchi ambayo Yahwe Mungu wako anawapatia kama urithi.

# 22

[1] Hautakiwi kumtazama ng'ombe au kondoo wa Muisraeli mwenzako akikosea
njia na ukajificha kwao; hakika unapaswa kuwarejesha kwake. [2] Iwapo Muisraeli
mwenzako hayupo karibu nawe, au kama haumfahamu, basi unapaswa kumleta
mnyama huyo nyumbani kwako, na lazima uwe naye mpaka pale mwenyewe

atakapomtafuta, na kisha lazima umrejeshee mwenyewe. 3 Unapaswa kufanya vivyo
hivyo kwa punda wake; unapaswa kufanya vivyo hivyo na vazi lake; unapaswa
kufanya vivyo hivyo kwa kila kitu alichopoteza Muisraeli mwenzako, kitu chochote
alichopoteza na ukakipata; hautakiwi kujificha. 4 Haupaswi kumwona punda wa
Muisraeli mwenzako au ng'ombe wake kaanguka chini barabarani na kujificha
dhidi yao; hakika unapaswa kumsaidia kumwinua tena. 5 Mwanamke hatakiwi
kuvaa kinachokusudiwa kwa mwanamume, vilevile mwanamume hapaswi kuvaa
mavazi ya mwanamke; kwa maana yeyote afanyaye vitu hivi ni chukizo kwa
Yahwe Mungu wako. 6 Iwapo kiota cha ndege kikaonekana barabarani mbele yako,
kwenye mti wowote au juu ya ardhi, kikiwa na makinda ya ndege au mayai ndani
mwake, na mama yao akiwa juu yao au juu ya mayai, haupaswi kumchukua mama
pamoja na makinda au mayai yake. 7 Hakika unapaswa kumuacha mama aende
zake, ila makinda yake unaweza kuyachukua. Tii amri hii ili uenende vyema, na
siku zako ziweze kurefushwa. 8 Ujengapo nyumba mpya, basi unapaswa kujenga
kitalu kwa ajili ya paa yako ili usilete damu juu ya nyumba yako mtu akianguka
kutoka pale. 9 Haupaswi kupanda shamba lako la mizabibu kwa mbegu mbili,
ili kwamba mavuno yote yasichukuliwe na sehemu takatifu, mbegu uliyoipanda
pamoja na matunda ya mzabibu. 10 Haupaswi kulimia ng'ombe na punda kwa
pamoja. 11 Haupaswi kuvaa kitambaa kilichotengenezwa kwa sufu na kitani kwa
pamoja. 12 Unapaswa kutengeneza pindo katika pembe nne za nguo unayoivaa.
13 Iwapo mwanamume kachukua mke, kisha kalala naye, na baadae kumchukia,
14 na kisha kumtuhumu kwa vitu vya aibu na kumharibia sifa yake kwa kusema,
"Nilimchukua huyu mwanamke, lakini nilipomkaribia sikukuta ushahidi waubikra
kwake". 15 Kisha baba na mama mzazi wa binti wanatakiwa kupeleka ushahidi
wa ubikra wake kwa wazee mlangoni mwa mji. 16 Baba wa binti anapaswa
kuwaambia wazee, "nilimpatia binti yangu kwa mwanamume huyu awe mkewe,
naye anamchukia. 17 Tazama, amemtuhumu na vitu vya aibu na kusema, "Sikukuta
ushahidi wa ubikra kwa binti yako". Lakini ushahidi huu hapa wa ubikra wa
binti yangu". Kisha watatandaza shuka mbele ya wazee wa mji. 18 Wazee wa
mji wanapaswa kumchukua mwanamume huyo na kumuadhibu; 19 nao wanapaswa
kumtoza faini ya shekeli mia moja ya fedha, na kumpatia baba wa binti, kwa sababu
mwanamume kasababisha sifa mbaya kwa bikra wa Israeli. Binti huyu anapaswa
kuwa mke wake; mwanamume huyu hatakiwi kumfukuza katika siku zake zote. 20 Ila
kama jambo hili ni la kweli, kwamba ushahidi wa bikra ya binti haukupatikana,
21 basi wanapaswa kumpeleka binti mlangoni kwa baba yake, na kisha wanamume
wa mji wake wanatakiwa kumpiga kwa mawe hadi afe, kwa sababu amefanya
jambo la aibu katika Israeli, kwa kutenda kama kahaba chini ya nyumba ya baba
yake, nanyi mtakuwa mmeondoa uovu miongoni mwenu. 22 Iwapo mwanamume
kakutwa analala na mwanamke ambaye ni mke wa mtu, basi wote wanapaswa
kufa, mwanamume aliyelala na mwanamke pamoja na mwanamke mwenyewe;
nanyi mtakuwa mmeondoa uovu miongoni mwenu. 23 Iwapo kuna msichana bikra,
ambaye amechumbiwa na mwanamume, kisha mwanamume mwingine kamkuta
mjini na kulala naye, 24 wachukueni wote wawili malangoni mwa mji, na kuwapiga
mawe. Unapaswa kumpiga msichana mawe, kwa sababu hakupaza sauti kuomba
msaada, ingawa alikuwa ndani ya mji. Unapaswa kumpiga mwanamume mawe,
kwa sababu amemwingilia mke wa jirani yake; nanyi mtakuwa mmeondoa uovu
miongoni mwenu 25 Lakini kama mwanamume amemkuta msichana aliyechumbiwa
shambani, na kama akamkamata na kulala naye, basi mwanamume pekee aliyelala
naye ndiye lazima afe. 26 Lakini kwake msichana msifanye chochote; hakuna dhambi
inayostahili kifo kwake msichana. Kwa maana suala hili ni kama mwanamume

amshambuliapo jirani yake na kumuua. 27 Kwa maana alimkuta shambani; msichana
huyu aliyechumbiwa alipaza sauti, lakini hapakuwa na mtu wa kumuokoa. 28 Iwapo
mwanamume amemkuta msichana ambaye ni bikra lakini hajachumbiwa, na kama
akamkamata na kulala naye, na kama wakagundulika, 29 basi mwanamume aliyelala
naye lazima atoe shekeli hamsini za fedha kwa baba wa msichana, naye lazima
awe mke wake, kwa sababu amemdhalilisha. Hatakiwi kumfukuza katika siku zake
zote. 30 Mwanamume hapaswi kumchukua mke wa baba yake kama wake; hatakiwi
kuchukua haki za ndoa za baba yake.

# 23

1 Mwanamume aliyejeruhiwa kwa kupondwa au kukatwa haruhusiwi kuingia
katika kusanyiko la Yahwe. 2 Mwana haramu haruhusiwi kuwa miongoni mwa
kusanyiko la Yahwe; kutoka hadi kizazi cha kumi cha uzao wake, hakuna kati yao
anatakiwa kuwa kwenye kusanyiko la Yahwe. 3 Muamori au Mmoabu haruhusiwi
kuwa miongoni mwa kusanyiko la Yahwe; kutoka hadi kizazi cha kumi cha uzao
wake, hakuna kati yao anatakiwa kuwa kwenye kusanyiko la Yahwe. 4 Hii ni kwa
sababu hawakukutana nanyi kwa mkate na maji barabarani mlipokuwa mmetoka
nje ya Misri, na kwa sababu walimkodisha Balaamu mwana wa Beoro kutoka Pethoro
kule Aramu Naharaimu, awalaani. 5 Lakini Yahwe Mungu wako hakumsikiliza
Balaamu; badala yake, Yahwe Mungu wako aligeuza laana kuwa baraka kwenu,
kwa sababu Yahwe Mungu wako aliwapenda. 6 Hamtakiwi kutafuta amani au
mafanikio yao, katika siku zenu zote. 7 Hutakiwi kumchukia Muedomi, kwa maana
ni kaka yako; hutakiwi kumchukia Mmisri, kwa maana ulikuwa mgeni katika nchi
yake. 8 Wazawa wa kizazi cha tatu wanaozaliwa kwao wanaweza kuwa katika
kusanyiko la Yahwe. 9 Utakapotembea kijeshi dhidi ya maadui zako, basi unapaswa
kujitenga na kila aina ya uovu. 10 Iwapo miongoni mwenu kuna mwanamume
ambaye sio msafi kwa sababu ya jambo lililofanyika kwake usiku, basi anatakiwa
atoke nje ya kambi ya jeshi; hatakiwi kurudi kambini. 11 Jioni ikifika, anatakiwa
ajiogeshe kwa maji; na jua likizama atarudi ndani kambini. 12 Pia unatakiwa kuwa
na eneo nje ya kambi ambayo utakwenda; 13 na utakuwa na kitu katika zana
zako cha kuchimbia; utakapochuchumaa kujisaidia, unapaswa kuchimbia nacho
na kisha kurudishia udongo na kufunika kile kilichotoka kwako. 14 Kwa maana
Yahwe Mungu wako anatembea miongoni mwa kambi yenu kuwapa ushindi na
kuwapa maadui zenu mkononi mwenu. Kwa hiyo kambi yenu lazima iwe takatifu, ili
kwamba asione kitu chochote kichafu miongoni mwenu na kuwaacha. 15 Hutakiwi
kumrudishia bwana mtumwa aliyetoroka kwake. 16 Mruhusu aishi pamoja nawe,
katika mji wowote atakaochagua. Usimuonee. 17 Hapatakiwi kuwa na kahaba wa
kidhehebu miongoni mwa mabinti wa Israeli, na wala hapatakiwi kuwa na kahaba
wa kidhehebu miongoni mwa wana wa kiume wa Israeli. 18 Hautakiwi kuleta
mshahara wa kahaba au mshahara wa mbwa katika nyumba ya Yahwe Mungu
wako kwa kiapo chochote; kwa maana vyote hivi na machukizo mbele ya Yahwe
Mungu wako. 19 Hutakiwi kumkopesha Muisraeli mwenzako kwa riba – riba ya
fedha, riba ya chakula, au riba ya kitu chochote kinachokopeshwa kwa riba. 20 Kwa
mgeni unaweza kukopesha kwa riba; lakini kwa Muisraeli mwenzako haupaswi
kukopesha kwa riba, ili kwamba Yahwe Mungu wako aweze kukubariki katika kila
jambo uwekalo mkono wako, katika nchi ambayo mnaenda kumiliki. 21 Unapofanya
kiapo kwa Yahwe Mungu wako, haupaswi kukawia kuikamilsha, kwa maana Yahwe
Mungu wako hakika atadai kiapo hicho; itakuwa dhambi kako usipokamilisha.
22 Lakini iwapo utajizuia kutoa kiapo, haitakuwa dhambi kwako. 23 Kile ambacho
kimetoka kinywani mwako unapaswa kukifuata na kukitekeleza; kulingana na kiapo

ulichotamka kwa Yahwe Mungu wako, chochote ulichotamka kwa hiari kwa kinywa
chako. [24] Utakapokwenda katika shamba la mizabibu la jirani yako, unatakiwa kula
mizabibu idadi yoyote unayotaka, lakini hautakiwi kuhifadhi yoyote katika kikapu
chako. [25] Utakapokwenda katika shamba la zao lililoiva la jirani yako, unaweza
kuvuna kichwa cha mavuno kwa mkono wako, lakini haupaswi kutumia mundu
kuvuna zao lililoiva la jirani yako.

# 24

[1] Mwanamume akimchukua mke na kumuoa, na mke asipokubalika machoni
pa mumewe kwa sababu kagundua jambo ambalo si jema kwake, basi anatakiwa
amwandikie talaka, aiweke mkononi mwake, na kumfukuza nyumbani kwake.
[2] Akishaondoka nyumbani kwake, anaweza kwenda na kuwa mke wa mwanamume
mwingine. [3] Iwapo mume wa pili akamchukia na kumwandikia talaka, akaiweka
mkononi mwake, na kumfukuza nyumbani kwake; au huyu mume wa pili akafariki,
mwanamume aliyemchukua kuwa mke wake – [4] basi mume wa awali, yule
aliyemfukuza mara ya kwanza, haruhusiwi kumchukua tena awe mke wake, baada
ya yeye kuwa mchafu, kwa maana hiyo itakuwa ni chukizo kwa Yahwe. Hautakiwi
kusababisha nchi iwe na hatia, nchi ambayo Yahwe Mungu wako anakupatia
kama urithi. [5] Mwanamume atakapochukua mke mpya, hatakwenda vitani na
jeshi, na wala hataamrishwa kwenda kwenye shughuli yoyote ya kulazimishwa;
atakuwa huru kuwa nyumbani kwa mwaka mzima na atamfurahisha mke wake
aliyemchukua. [6] Mwanamume yeyote hatachukua kinu wala jiwe la kinu kama
dhamana, kwa maana hivyo itakuwa kuchukua Maisha ya mtu kama dhamana.
[7] Iwapo mwanamume kakutwa kamteka mmoja wa kaka zake miongoni mwa watu
wa Israeli, na kumtendea kama mtumwa na kisha kumuuza, huyo mwizi lazima
afe; na utakuwa umeondoa uovu miongoni mwenu. [8] Kuwa mwangalifu kuhusu
kiini chochote cha ukoma, ili kwamba uwe makini katika kuchunguza na kufuata
kila agizo linalopewa kwako ambalo makuhani, Walawi, wanakufundisha; kama
nilivyowaamuru, ili utekeleze. [9] Kumbukeni nini Yahwe Mungu wako alichomfanya
Miriam ulipokuwa ukitoka Misri. [10] Utoapo mkopo wa aina yoyote kwa jirani yako,
hautakiwi kwenda ndani ya nyumba yake kutafuta dhamana yake. [11] Utasimama
nje, na mwanamume aliyekopa kwako ataleta dhamana yake nje kwako. [12] Iwapo ni
mtu maskini, hautakiwi kulala na dhamana yake ikiwa mikononi mwako. [13] Hakika
unapaswa kumrejeshea dhamana yake kabla jua halijazama, ili aweze kulala ndani
ya vazi lake na akubariki; itakuwa utakatifu kwako mbele za Yahwe Mungu wako.
[14] Hautakiwi kumuonea mtumishi wa kuajiriwa ambaye ni maskini na mhitaji, hata
kama ni jamaa wa Israeli, au ni kati ya wageni mbao wamo katika nchi ndani ya
malango ya mji wako; [15] Kila siku unapaswa kumlipa mshahara wake; jua halipaswi
kuzama kabla ya suala hili kutatuliwa, kwa maana ni maskini na anautegemea.
Fanya hivi ili asilie dhidi yako kwa Yahwe, na kwamba isiwe ikawa dhambi ambayo
umeitenda. [16] Wazazi hawapaswi kuuwawa kwa niaba ya watoto wao, na wala
watoto hawapaswi kuuawa kwa niaba ya wazazi wao. Badala yake, kila mtu
anapaswa kuuwawa kwa dhambi yake mwenyewe. [17] Haupaswi kutumia nguvu
kuchukua haki inayomhusu mgeni au yatima, wala kuchukua vazi la mjane kama
dhamana. [18] Badala yake, unapaswa ukumbuke ya kwamba ulikuwa mtumwa Misri,
na kwamba Yahwe Mungu wako alikukomboa kutoka kule. Kwa hiyo ninakuagiza
kutii amri hii. [19] Utakapovuna zao lako shambani mwako, na ukasahau kipande
cha mbegu shambani, haupaswi kurudi na kukichukua; kinapaswa kuwa cha mgeni,
cha yatima, au cha mjane, ili Yahwe Mungu wako akubariki katika kazi ya mikono
yako. [20] Utakapotikisa mti wako wa mzeituni, haupaswi kupanda juu ya matawi

tena; itakuwa kwa ajili ya mgeni, kwa yatima na kwa mjane. [21] Utakapokusanya
mizabibu shambani mwako, haupaswi kukusanya masazo yake tena. Kinachobaki
kitakuwa cha mgeni, cha yatima na cha mjane. [22] Unatakiwa ukumbuke kuwa
ulikuwa mtumwa katika nchi ya Misri; kwa hiyo nakuagiza kutii amri hii.

## 25

[1] Iwapo kutakuwa na malumbano kati ya wanaume na wakaenda mahakamani, na
waamuzi wakawahukumu, basi watamwachilia mtakatifu na kumhukumu muovu.
[2] Iwapo mwanamume mwenye hatia anastahili kupigwa, basi muamuzi atamfanya
alale chini na kupigwa mbele zake kwa idadi iliyoamriwa kulingana na kosa lake.
[3] Muamuzi anaweza kumpatia mapigo arobaini, lakini hapaswi kuvuka idadi hiyo;
kwa maana akivuka idadi hiyo na kumpiga kwa mapigo mengi zaidi, basi Muisraeli
mwenzako atakuwa kaaibishwa mbele ya macho yenu. [4] Haupaswi kumfunga punda
wako pua na mdomo anapokuwa akilima shamba lako. [5] Iwapo kaka wanaishi
pamoja na mmoja wao akafariki bila kuwa na mwana, basi mke wa marehemu
hatakiwi kuolewa na mtu nje ya familia. Badala yake, kaka yake mumewe anapaswa
kulala naye na kumchukua kuwa mke wake na kutekeleza wajibu wa kaka wa mume
kwake. [6] Hii ni kwamba mtoto wa kwanza atakayezaliwa arithi chini ya jina la kaka
yake mwanamume aliyefariki, ili jina lake lisiangamie ndani ya Israeli. [7] Lakini
kama mwanamume hataki kumchukua mke wa kaka yake awe wake, basi mke wa
kaka yake anapaswa kwenda malangoni mpaka kwa wazee na kusema, "Kaka wa
mume wangu amekataa kuwajibika kwa niaba ya jina la kaka yake humu Israeli;
hataki kufanya wajibu wa kaka wa mume kwangu". [8] Kisha wazee wa mji wake
wanapaswa kumuita na kuzungumza naye. Lakini tuseme atasisitiza na kusema,
"Sitaki kumchukua". [9] Basi mke wa kaka yake anatakiwa kuja kwake mbele ya wazee,
kumvua ndara zake miguuni mwake, na kumtemea usoni. Anapaswa kumjibu na
kusema, "Hivi ndivyo kinachofanyika kwa mwanamume asiyetaka kujenga nyumba
ya kaka yake". [10] Jina lake Israeli litaitwa, "Nyumba ya mtu aliyevuliwa ndara
zake". [11] Iwapo wanamume wamepigana wao kwa wao, na mke wa mmoja wao
kaja kumkomboa mumewe dhidi ya yule aliyempiga, naye akanyosha mkono wake na
kumshika sehemu za siri, [12] basi unapaswa kuukata mkono yake; jicho lako halipaswi
kuwa na huruma. [13] Haupaswi kuwa na mizani ya uzito tofauti katika mfuko wako,
mkubwa na mdogo. [14] Hautakiwi kuwa na vipimo tofauti ndani ya nyumba yako,
vikubwa na vidogo. [15] Unatakiwa kuwa na uzito kamili na wa haki; unatakiwa
kuwa na vipimo kamili na vya haki, ili siku zako ziwe ndefu katika nchi ambayo
Yahwe Mungu wako anakupatia. [16] Kwa maana wote wanaofanya vitu hivi, wote
wanaovunja haki, ni chukizo kwa Yahwe Mungu wako. [17] Kumbuka ni jambo gani
Amaleki alichofanya kwako barabarani ulipokuwa ukitoka Misri, [18] jinsi alivyokutana
na wewe barabarani na kuwashambulia kati yenu kwa nyuma, wale waliokuwa
wamelegea nyuma, mlipokuwa dhaifu na kuchoka, hakumheshimu Mungu. [19] Kwa
hiyo, Yahwe Mungu wako atakapowapa pumziko kutoka kwa maadui zako kila
sehemu, katika nchi ambayo Yahwe Mungu wako anawapatia kumiliki kama urithi,
hautakiwi kusahau kuwa unapaswa kufuta kumbukumbu ya Waamaleki chini ya
mbingu.

## 26

[1] Utakapofika katika nchi ambayo Yahwe Mungu wako anakupatia kama urithi, na
utakapoimiliki na kuishi ndani yake, [2] basi unatakiwa kuchukua baadhi ya mavuno
yote ya kwanza ya ardhi uliyoyaleta kutoka katika nchi ambayo Yahwe Mungu wako
anakupatia. Unatakiwa kuyaweka ndani ya kikapu na kuelekea katika eneo ambalo

Yahwe Mungu wako atapachagua kama mahali patakatifu. [3] Unatakiwa kwenda kwa
kuhani ambaye atakuwa akihudumu katika siku hizo na kumwambia, “Siku ya leo
ninakiri kwa Yahwe Mungu wako ya kuwa nimekuja katika nchi ambayo Yahwe
aliapa kwa mababu zetu kutupatia”. [4] Kuhani anatakiwa kuchukua kikapu mkononi
mwako na kukiweka madhabahuni ya Yahwe Mungu wako. [5] Unapaswa kusema
mbele ya Yahwe Mungu wako, “Babu yangu alikuwa Mwaremi mzururaji. Alikwenda
chini hadi Misri na kukaa kule, na idadi ya watu wake ilikuwa chache. Kule akawa
taifa kubwa, lenye nguvu na idadi kubwa. [6] Wamisri walitutendea vibaya na kututesa.
Walitulazimisha kufanya kazi za watumwa. [7] Tulimlilia Yahwe, Mungu wa baba zetu,
naye akasikia sauti yetu na kuona mateso yetu, kazi zetu na mateso yetu. [8] Yahwe
alituondoa Misri kwa mkono wake mkuu, kwa mkono wake ulionyoshwa, kwa hofu
kuu, kwa ishara na miujiza; [9] na ametuleta katika sehemu hii na kutupatia nchi hii,
nchi inayotiririka kwa maziwa na asali. [10] Tazama sasa, nimeleta mavuno ya kwanza
kutoka katika nchi ambayo wewe, Yahwe, umenipatia. ” Unapaswa kuweka chini
mbele ya Yahwe Mungu wako na kuabudu mbele zake; [11] na unapaswa kufurahia
katika mema yote ambayo Yahwe Mungu wako amekufanyia, kwa ajili na nyumba
yako – wewe, na Mlawi, na mgeni aliye miongoni mwako. [12] Utakapomaliza kutoa
zaka yote ya mavuno katika mwaka wa tatu, yaani, mwaka wa kutoa zaka, basi
unapaswa kuwapatia Mlawi, kwa mgeni, kwa yatima, na kwa mjane, ili kwamba
waweze kula ndani ya malango yenu ya mji na kujazilishwa. [13] Unatakiwa kusema
mbele ya Yahwe Mungu wako, “Nimetoa kutoka nyumbani mwangu vitu ambavyo ni
mali ya Yahwe, na kumpatia Mlawi, mgeni, yatima, na mjane, kulingana na amri zote
ulizonipatia. Sijavunja amri yako yoyote, wala sijazisahau. [14] Sijala kati yao wakati
wa maombolezo yangu, wala sijaziweka mahali pengine nilipokuwa mchafu, wala
sijazitoa kati yao kwa heshima ya wafu. Nimesikiliza sauti ya Yahwe Mungu wangu;
Nimetii kila kitu ulichoniamuru kukifanya. [15] Tazama chini kutoka mahali patakatifu
unapoishi, kutoka mbinguni, na ubariki watu wako Israeli, na nchi uliyotupatia,
kama ulivyoapa kwa mababu zetu, nchi inayotiririka kwa maziwa na asali. [16] Leo
Yahwe Mungu wako anawaamuru kuzitii sheria na amri hizi; basi utazishikilia na
kuzitenda kwa moyo wako wote na kwa nafsi yako yote. [17] Umetamka leo ya kuwa
Yahwe ni Mungu wako, na kwamba utatembea katika njia zake na kushikilia sheria
zake, maagizo yake na amri zake, na kwamba utaisikiliza sauti yake. [18] Leo Yahwe
ametamka ya kwamba mu watu ambao ni mali yake, kama alivyoahidi kwenu, na
kwamba mnapaswa kushikilia amri zake zote. [19] Na atawaweka juu zaidi ya mataifa
mengine aliyoyaumba nanyi mtapokea sifa, umaarufu na heshima. Mtakuwa watu
waliowekwa kando kwa Yahwe Mungu wako, kama alivyosema.”

# 27

[1] Musa na wazee wa Israeli waliwaamuru watu na kusema, “Zishikeni amri zote
ninazowaamuru leo. [2] Katika siku mtakapopita juu ya Yordani kwenye nchi ambayo
Yahwe Mungu wako anawapatia, mnapaswa kutengeneza mawe kiasi makubwa na
kuyachapa kwa lipu. [3] Mnatakiwa kuyaandika juu yake maneno yote ya sheria
hii pale mtakapovuka; ili muweze kwenda katika nchi ambayo Yahwe Mungu
wako anawapatia, nchi inayotiririka kwa maziwa na asali, kama Yahwe, Mungu
wa mababu zenu, alivyowaahidi. [4] Mtakapovuka juu ya Yordani, yapangane haya
mawe ninayowaamuru leo, juu ya mlima wa Ebali, na myapige kwa lipu. [5] Hapo
mnapaswa kujenga dhabahu kwa Yahwe Mungu wako, dhabahu la mawe; lakini
hautakiwi kuinua chombo cha chuma kujenga mawe. [6] Unatakiwa kujenga dhabahu
ya Yahwe Mungu wako kwa mawe yasiyokuwa na kazi; unatakiwa kutoa dhabihu
ya kuteketeza juu yake kwa Yahwe Mungu wako, [7] na utatoa sadaka ya pamoja na

utakula pale; utafurahia mbele ya Yahwe Mungu wako. 8 Utaandika juu ya mawe
maneno yote ya sheria hii kwa wazi. 9 Musa na makuhani, Walawi, waliongea na
Waisraeli wote na kusema, “Nyamazeni na sikilizeni Israel: Leo mmekuwa watu
wa Yahwe Mungu wenu. 10 Mnapaswa basi kutii sauti ya Yahwe Mungu wenu na
kutii amri na sheria zake ambazo ninawaamuru leo.” 11 Musa aliwaamuru watu
siku hiyo hiyo na kusema, 12 “Makabila haya yanapaswa kusimama katika mlima
Gerizimu kuwabariki watu baada ya nyinyi kuvuka Yordani; Simeoni, Lawi, Judah,
Isakari, Yusufu na Benyamini. 13 Haya ni makabila ambayo lazima yasimame juu
yam lima Ebali kutamka laana: Rubeni, Gadi, Asheri, Zabuloni, Dan na Naftali.
14 Walawi watajibu na kusema kwa wanamume wote wa Israeli kwa sauti kubwa:
15 “Alaaniwe mwanamume atakayechonga sanamu au kinyago, chukizo kwa Yahwe,
kazi ya mikono ya fundi, ambayo ataifanya sirini”. Kisha watu wote wanapaswa
kujibu na kusema, ‘Amina’. 16 Alaaniwe mwanamume atakayemuaibisha baba yake
au mama yake. Kisha watu wote waseme, 'Amina'. 17 Alaaniwe mwanamume
anayetoa alama ya ardhi.' Kisha watu wote na waseme, 'Amina'. 18 Alaaniwe
mwanamume asababishae kipofu kutoka nje ya barabara. Kisha watu wote waseme,
‘Amina’. 19 Alaaniwe mwanamume atumiaye nguvu kupokonya haki inayomstahili
mgeni, yatima, au mjane. Kisha watu wote lazima waseme, ‘Amina’. 20 Alaaniwe
mwanamume atakayelala na mke wa baba yake, kwa sababu atakuwa amechukua
haki za baba yake’. Kisha watu wote lazima waseme, ‘Amina’. 21 Alaaniwe
mwanamume atakayelala na aina yoyote ya mnyama’. Kisha watu wote lazima
waseme, ‘Amina’. 22 Alaaniwe mwanamume atakayelala na dada yake, binti wa
baba yake, au binti wa mama yake. Kisha watu wote lazima waseme, ‘Amina’.
23 Alaaniwe mwanamume atakayelala na mama mkwe’. Kisha watu wote lazima
waseme, ‘Amina’. 24 Alaaniwe mwanamume atakayemuua jirani yake kwa siri’.
Kisha watu wote lazima waseme, ‘Amina’. 25 Alaaniwe mwanamume apokeaye
rushwa kumuua mtu asiye na hatia’. Kisha watu wote lazima waseme, ‘Amina’.
26 Alaaniwe mwanamume asiyethibitisha maneno ya sheria hii, ili kwamba ayatii. ’
Kisha watu wote lazima waseme, ‘Amina’.

# 28

1 Utakaposikiliza kwa makini sauti ya Yahwe Mungu wako ili kwamba ushikilie
amri zake zote ambazo nakuamuru leo, Yahwe Mungu wako atakuweka juu ya
mataifa yote ya ulimwengu. 2 Baraka hizi zote zitakuja kwako na kukupita, kama
utasikiliza sauti ya Yahwe Mungu wako. 3 Utabarikiwa ndani ya mji, na utabarikiwa
shambani. 4 Matunda ya mwili wako yatabarikiwa, na matunda ya ardhi yako,
na matunda ya wanyama wako, ongezeko la ng’ombe wako, na wachanga wa
mifugo wako. 5 Kitabarikiwa kikapu chako na chombo cha kukandia. 6 Utabarikiwa
utakaporudi ndani, na utabarikiwa utakapotoka nje. 7 Yahwe atasababisha maadui
zako wanaoinuka dhidi yako kupigwa chini mbele yako; watajitokeza dhidi yako kwa
njia moja lakini watakimbia mbele zako kwa njia saba. 8 Yahwe ataamuru baraka
kuja kwako katika maghala yako na katika kila unapoweka mkono wako; atakubariki
katika nchi anayokupatia. 9 Yahwe atawaimarisha kama watu waliotengwa kwa
ajili yake, kama alivyoapa kwenu, iwapo mtashikilia amri za Yahwe Mungu wenu,
na kutembea katika njia zake. 10 Watu wote wa ulimwengu wataona ya kwamba
mmeitwa kwa jina la Yahwe, nao watawaogopa. 11 Yahwe atakufanya kuwa na
mafanikio sana katika matunda ya mwili wako, katika matunda ya ng’ombe zako,
katika matunda ya ardhi yako, katika nchi aliyoapa kwa mababu zako kuwapatia.
12 Yahwe atafungua kwako ghala lake la mbingu kuruhusu mvua juu ya ardhi
katika muda sahihi, na kubariki kazi zote za mikono yako; utakopesha kwa mataifa

mengi, lakini wewe hautakopa. 13 Yahwe atakufanya kuwa kichwa, na sio mkia;
utakuwa juu tu, na hautakuwa chini, iwapo utaisikiliza amri za Yahwe Mungu
wako ambazo ninakuamuru leo, ili kuzishikilia na kuzitenda, 14 na usipogeuka
kinyume na maneno yoyote ninayokuamuru leo, kulia kwako wala kushoto kwako,
na kufuata miungu mingine na kuwatumikia. 15 Lakini usiposikiliza sauti ya Yahwe
Mungu wako, na kushikilia amri zake zote na sheria zake ninazokuamuru leo, basi
laana hizi zote zitakuja kwako na kukupita. 16 Utalaaniwa utakapokuwa mjini, na
utalaaniwa utakapokuwa shambani. 17 Kitalaaniwa kikapu chako na chombo chako
cha kukandia. 18 Litalaaniwa tunda la mwili wako, tunda la ardhi yako, ongezeko la
ng'ombe wako, na wachanga wa mifugo. 19 Utalaaniwa utakaporudi, na utalaaniwa
utokapo. 20 Yahwe atatuma laana juu yako, kuchanganyikiwa, na shutuma katika
kila jambo uwekalo mikono yako, hadi utakapoangamizwa, na hadi utakapotoweka
haraka kwa sababu ya matendo yako maovu ambayo utakuwa umenitelekeza mimi.
21 Yahwe atafanya pigo likung'ang'anie mpaka kukuangamiza kutoka katika nchi
utakayoenda kumiliki. 22 Yahwe atakushambulia kwa magonjwa ya kuambukiza, kwa
homa, kwa uvimbe, na kwa kiangazi na jua kali, na kwa upepo mkali na ukungu.
Hivi vitakufukuza hadi uangamie. 23 Mbingu zilizo juu ya vichwa vyenu zitakuwa
shaba, na ardhi chini yenu itakuwa chuma. 24 Yahwe atafanya mvua ya ardhi yako
kuwa unga na vumbi, kutoka mbinguni vitashuka kwako, hadi utakapoangamizwa.
25 Yahwe atakusababishia upigwe mbele ya maadui zako; utawafuata kwa njia
moja dhidi yao lakini utakimbia mbele zao kwa njia saba. Utapelekwa huku
na kule miongoni mwa falme za nchi. 26 Mzoga wako utakuwa chakula kwa
ndege wote wa angani na kwa wanyama wa ulimwengu; hakutakuwa na mtu wa
kuwatisha. 27 Yahwe atawashambulia na majipu ya Misri na vidonda, kiseyeye na
mwasho ambazo hautapona. 28 Yahwe atakushambulia kwa ukichaa, kwa upofu,
pamoja na kuchanganyikiwa kwa akili. 29 Utapapasa papasa mchana kama kipofu
apapasavyo usiku, na hautafanikiwa katika njia zako; daima utakandamizwa na
kuporwa, na hakutakuwa na mtu wa kukuokoa. 30 Utamchumbia mwanamke, lakini
mwanamume mwingine atamkamata na kumbaka. Utajenga nyumba lakini hautaishi
ndani mwake; utapanda shamba la mizabibu lakini hautafurahia matunda yake.
31 Ng'ombe wako atachinjwa mbele ya macho yako, lakini hautakula nyama yake;
punda wako atachukuliwa kwa nguvu mbele yako na hatarejeshwa kwako. Kondoo
wako watapewa maadui zako, na hautakuwa na mtu wa kukusaidia. 32 Watoto wa
kiume na mabinti zako watapewa kwa watu wengine; macho yako yatawatafuta siku
nzima, lakini yatashindwa kwa shauku juu yao. Hakutakuwa na nguvu mikononi
mwako. 33 Mavuno ya ardhi yako na ya kazi yako yote – taifa usilolijua litayatafuna;
daima utaonewa na kugandamizwa, 34 ili upatwe na wazimu kwa yale utakayoona
yakitendeka. 35 Yahwe atakushambulia kwenye magoti na miguu kwa majibu makali
ambayo hutaweza kupona, kutoka chini ya miguu yako mpaka juu ya kichwa chako.
36 Yahwe atawachukua pamoja na mfalme ambaye mtakuwa mmemuweka juu yenu
kwa taifa ambalo hamjalijua, wala nyie au mababu zenu; kule mtaabudu miungu
mingine ya mbao na mawe. 37 Nawe utakuwa chanzo cha kitisho, mithali, na
uvumi, miongoni mwa watu wote ambako Yahwe atakupeleka. 38 Utaweka mbegu
nyingi shambani, lakini utakusanya mbegu chache, kwa maana nzige itaziangamiza.
39 Utapanda mashamba ya mizabibu na kuyapalilia, lakini hautakunywa divai yoyote,
wala hautakusanya matunda yoyote, kwa maana funza watayala. 40 Utakuwa na
miti ya mizeituni katika eneo lako, lakini hautajipaka mafuta yoyote juu yako, kwa
maana mti wako wa mzeituni utaangusha matunda yake. 41 Utakuwa na wana wa
kiume na mabinti, lakini hawatabaki kuwa wako, kwani watachukuliwa mateka.
42 Miti yako yote na matunda ya ardhi yako – nzige watajitwalia. 43 Mgeni aliye

miongoni mwako atainuka juu zaidi yako juu na juu; wewe mwenyewe utashuka
chini na chini. 44 Atakukopesha, lakini hautamkopesha; atakuwa kichwa, nawe
utakuwa mkia. 45 Laana hizi zote zitakujia juu yako na kukuandama na kukupita
hadi utakapoangamizwa. Hii itatokea kwa sababu haukuisikia sauti ya Yahwe
Mungu wako, ili kushikilia amri na maagizo yake aliyokuamuru. 46 Laana hizi
zitakuwa juu yako kama ishara na miujiza, na juu ya uzao wako milele. 47 Kwa
sababu hukumuabudu Yahwe Mungu wako kwa shangwe na furaha moyoni mwako
ulipokuwa na mafanikio, 48 kwa hiyo utatumikia maadui ambao Yahwe atatuma
dhidi yako; utawatumikia katika njaa, katika kiu, katika uchi, na katika umaskini.
Ataweka mzigo wa chuma juu ya shingo yako hadi akuangamize. 49 Yahwe ataleta
taifa dhidi yako kutoka mbali, kutoka mwisho wa ulimwengu, kama tai arukaye kwa
mhanga wake, taifa ambalo lugha yake hauelewi; 50 taifa lenye sura katili ambalo
haliheshimu wazee na halionyeshi fadhila kwa wadogo. 51 Watakula wachanga wa
ng'ombe wako na matunda ya ardhi yako hadi utakapoangamizwa. Hawatawaachia
nafaka, divai mpya, au mafuta, wachanga wa ng'ombe au mifugo yako, hadi
watakaposababisha kutoweka kwako. 52 Watawazingira katika malango ya miji yenu,
hadi kuta zenu ndefu na imara zitakaposhuka chini ardhini, kuta ambazo mliziamini.
Watawazingira ndani ya malango ya miji yenu kotekote katika nchi ambayo Yahwe
Mungu wenu amewapatia. 53 Utakula tunda la mwili wako mwenyewe, nyama
ya watoto wa kiume na binti zako, ambao Yahwe Mungu wako aliwapatia, katika
uvamizi na katika dhiki ambayo adui zako wataweka juu yako. 54 Mwanamume laini
na mlegevu miongoni mwenu – atakuwa na wivu kwa kaka yake na kwa mkewe, na
kwa watoto wowote waliosalia. 55 Kwa hiyo hatawapatia kati yao nyama ya watoto
wake ambayo ataenda kuila, kwa sababu hatabakiwa na chochote katika uvamizi
na dhiki ambayo adui yako ataiweka juu yako ndani ya malango yote ya mji wako.
56 Mwanamke laini na mlegevu miongoni mwenu, ambaye hatadiriki kuweka tako
la mguu wake ardhini kwa sababu ya ulaini na maringo yake – atakuwa na wivu
kwa mume kipenzi wake mwenyewe, kwa mtoto wake wa kiume, na kwa binti
yake, 57 na kwa mtoto wake mchanga atakayetoka katikati ya miguu yake, na kwa
watoto atakayewazaa. Atawala kwa siri kwa kukosa kitu kingine, katika uvamizi na
dhiki ambayo adui yako ataweka juu yako ndani ya malango ya mji wako. 58 Iwapo
hautashika maneno yote ya sheria yaliyoandikwa katika kitabu hiki, ili kuheshimu
jina hili tukufu na la kutisha, Yahwe Mungu wako, 59 basi Yahwe atafanya mapigo
yako kuwa ya kutisha, na yale ya wazao wako; yatakuwa mapigo makuu, ya muda
mrefu, na magonjwa makali, ya muda mrefu. 60 Ataleta juu yako mara nyingine
magonjwa yote ya Misri ambayo ulikuwa unayaogopa; yatakung'ang'ania. 61 Pia
kila gonjwa na pigo ambalo halijaandikwa katika kitabu cha sheria hii, hayo pia
Yahwe atayaleta juu yako hadi utakapoangamizwa. 62 Utabaki wachache kwa idadi,
ingawa ulikuwa kama nyota wa mbinguni kwa idadi, kwa sababu haukuisikiliza
sauti ya Yawhe Mungu wako. 63 Kama vile hapo awali Yawhe alivyofurahia juu yako
na kutenda mema, na kuwazidisha, basi atafurahia juu yako kwa kufanya upotee
na kwa kukuangamiza. Utang'olewa katika nchi utakayoenda kuimiliki. 64 Yahwe
atakusambaza miongoni mwa watu wote kutoka mwisho mmoja wa dunia hadi
mwisho mwingine wa dunia; huko utaabudu miungu mingine ambayo hujawajua,
wewe wala mababu zako, miungu ya mbao na jiwe. 65 Miongoni mwa mataifa
haya hautapata utulivu, na hakutakuwa na pumziko chini ya miguu yako; badala
yake, Yahwe atakupatia huko moyo wa kutetemeka, macho yanayofeli na nafsi
inayoomboleza. 66 Maisha yako yataning'inia kwa mashaka mbele yako; utaogopa
kila usiku na mchana na hutakuwa na uhakika kabisa maishani mwako. 67 Asubuhi
utasema, "Natamani ingekuwa jioni! " na jioni utasema, "Natamani ingekuwa

asubuhi! ” kwa sababu ya hofu mioyoni mwenu na vitu ambavyo macho yako
italazimu kuona. [68] Yahwe atakuleta Misri mara nyingine kwa meli, kwa njia ambayo
nilikuambia, “Hutaiona Misri tena”. Kule utajitoa kuuzwa kwa maadui zako kama
watumwa wa kiume na kike, lakini hakutakuwa na mtu wa kuwanunua.

# 29

[1] Haya ni maneno ambayo Yahwe alimuamuru Musa kuwaambia watu wa Israeli
katika nchi ya Moabu, maneno ambayo yaliongezwa katika agano alilolifanya pamoja
nao kule Horebu. [2] Musa aliwaita Waisraeli wote na kuwaambia, “Mmeona kila kitu
ambacho Yahwe alifanya mbele ya macho yenu katika nchi ya Misri kwa Farao,
kwa watumishi wake wote, na kwa nchi yake yote – [3] mateso makubwa ambayo
macho yenu yaliona, ishara, pamoja na ile miujiza mikubwa. [4] Lakini mpaka leo
Yahwe hajawapatia moyo wa kufahamu, macho ya kuona, au masikio ya kusikia.
[5] Nimewaongoza kwa miaka arobaini jangwani; mavazi yenu hayakuchakaa juu
yenu, na ndala zenu hazikuchakaa miguuni mwenu. [6] Hamkula mkate wowote,
na wala hamkunywa divai yoyote au kinywaji chochote chenye ulevi, ili kwamba
muweze kujua kuwa mimi ni Yahwe Mungu wenu. [7] Mlipokuja mahali hapa, Sihoni,
mfalme wa Heshboni, na Ogu, mfalme wa Bashani, walikuja dhidi yetu kutupiga,
na tukawapiga. [8] Tulichukua ardhi yao na kuwapa kama urithi Wareubeni, kwa
Wagadi, na kwa nusu ya kabila ya Manase. [9] Kwa hiyo shikilia maneno ya agano
hili na kuyatenda, ili ufanikiwe katika kila kitu ufanyacho. [10] Nyie wote, mnasimama
leo, mbele ya Yahwe Mungu wenu; machifu wenu, makabila yenu, wazee wenu, na
maafisa wenu – wanaume wote wa Israeli, [11] watoto wenu, wake zenu, na wageni
ambao wamo miongoni wa kambi yenu, kutoka kwa yule anayekata mbao zenu
mpaka kwa yule atekaye maji. [12] Mpo hapa ili kwamba muingie katika agano la
Yahwe Mungu wenu na katika kiapo ambacho Yahwe Mungu wako anafanya na
wewe leo, [13] ili kwamba awafanye leo kuwa watu wake, na kwamba aweze kuwa
Mungu kwa ajili yako, kama alivyonena kwako, na kama alivyoapa kwa mababu
zako, kwa Abrahamu, kwa Isaka na kwa Yakobo. [14] Kwa maana ninafanya agano hili
na kiapo hiki sio na wewe tu – [15] pamoja kila mtu aliyesimama hapa pamoja nasi
leo mbele ya Yahwe Mungu wetu – bali na wale ambao hawapo pamoja nasi leo pia.
[16] Unajua jinsi tulivyoishi katika nchi ya Misri, na jinsi tulivyopenya miongoni mwa
mataifa ambao uliwapita. [17] Mmeona sanamu zao zinazokera zilizotengenezwa kwa
mbao na mawe, fedha na dhahabu, ambazo zilikuwa miongoni mwenu. [18] Hakikisha
hakuna kati yenu mwanamume, mwanamke, ukoo, au kabila ambaye moyo wake
unamuacha Yahwe Mungu wetu leo, ili kwenda na kuabudu miungu ya mataifa hayo.
Hakikisha hakuna kati yenu mzizi utakaozaa nyongo na pakanga. [19] Wakati mtu huyo
anaposikia maneno ya laana hii, atajifariji moyoni mwake na kusema, “Nitakuwa na
amani, ingawa natembea katika ukaidi wa moyo wangu”. Hii itaangamiza ubichi
pamoja na ukavu. [20] Yahwe hatamsamehe, lakini badala yake, hasira ya Yahwe
na wivu wake utambanika mtu huyo, na laana zote zilizoandikwa katika kitabu
hiki vitakuwa juu yake, na Yahwe ataliondoa jina lake kutoka mbinguni. [21] Yahwe
atamuweka kando kwa ajili ya maafa kutoka katika makabila yote ya Israeli, kwa
kuzingatia laana zote za agano ambazo zimeandikwa katika kitabu hiki cha sheria.
[22] Kizazi kifuatacho, watoto wako watakaoinuka baada yako, na mgeni atakayekuja
kutoka nchi ya mbali, watazungumza watakapoona mapigo juu ya nchi hii na
magonjwa ambayo Yahwe ameyafanya yawe – [23] na watakapoona kuwa nchi yote
imekuwa salfa na chumvi ichomayo, ambapo hakuna kitu kipandwacho au kuzaa
matunda, ambapo hapaoti mmea wowote, kama anguko la Sodoma na Gomora,
Adma na Seboimu, ambayo Yahwe aliangamiza katika ghadhabu na hasira yake

– [24] watasema kwa pamoja na mataifa mengine, “Kwa nini Yahwe amefanya hili
katika nchi hii? Joto ya hasira hii kali inamaanisha nini?” [25] Kisha watu watasema,
“Ni kwa sababu walitelekeza agano la Yahwe, Mungu wa mababu zao, alilofanya
nao alipowatoa kutoka Misri, [26] na kwa sababu waliondoka na kutumikia miungu
mingine na kuzisujudu, miungu ambayo hawakujiua na ambayo hakuwapatia. [27] Kwa
hiyo hasira ya Yahwe imewaka dhidi ya nchi hii, ili kuleta juu yake laana zote
zilizoandikwa katika kitabu hiki. [28] Yahwe amewang'oa kutoka nchini kwao kwa
hasira, kwa ghadhanu, na kwa ghadhabu kali, na kuwatupa katika nchi nyingine,
leo. [29] Mambo ya siri ni ya Yahwe Mungu wetu pekee; lakini mambo yaliyofichuliwa
ni ya kwetu milele pamoja na wazawa wetu, ili tufanye maneno yote ya sheria hii.

# 30

[1] Vitu hivi vitakavyokuja juu yako, baraka na laana nilizoziweka mbele yako,
na utakapozirejea akilini miongoni mwa mataifa mengine ambapo Yahwe Mungu
wako kawapeleka, [2] na utakapomrudia Yahwe Mungu wako na kutii sauti yake, na
kufuata yote ambayo nayokuamuru leo – wewe na watoto wako – kwa moyo wako
wote na kwa nafsi yako yote, [3] kisha Yahwe Mungu wako atageuza kutekwa kwako
na kukuhurumia; atawarudisha na kuwakusanya kutoka kwa watu wote ambapo
Yahwe Mungu wako aliwatawanya. [4] Iwapo yeyote ya watu walio uhamishoni wapo
katika sehemu za mbali sana chini ya mbingu, kutoka huko Yawhe Mungu wako
atawakusanya, na kutoka huko atawarejesha. [5] Yahwe Mungu wako atawaleta katika
nchi ambayo mababu zenu walimiliki, nanyi mtaimiliki tena; atawatendea mema na
kuwazidisha zaidi ya alivyofanya kwa mababu zenu. [6] Yahwe Mungu wako atatahiri
moyo wako na moyo wa uzao wako, ili umpende Yahwe Mungu wako kwa moyo
wako wote na kwa nafsi yako yote, ili kwamba uweze kuishi. [7] Yahwe Mungu
wako ataweka laana hizi zote kwa maadui zako na kwa wote wakuchukiayo, wale
waliokutesa. [8] Utarudi na kutii sauti ya Yahwe, nawe utatenda amri zake zote ambazo
ninakuamuru leo. [9] Yahwe Mungu wako atakufanikisha katika kazi yote ya mkono
wako, katika matunda ya mwili wako, katika matunda ya mifugo yako, na katika
matunda ya nchi yako, kwa mafanikio; kwa maana Yahwe atafurahia tena mafanikio
yako, kama alivyofurahia kwa baba zako. [10] Atafanya hivi iwapo utatii sauti ya Yahwe
Mungu wako, ili kuzishika amri zake na kanuni zake zilizoandikwa katika kitabu hiki
cha sheria, iwapo utamgeukia Yahwe Mungu wako kwa moyo wako wote na kwa nafsi
yako yote. [11] Kwa maana amri hii nayokuamuru leo sio ngumu sana, wala haipo nje
ya uwezo wako kufikia. [12] Haipo mbinguni, ili usije ukasema, “Nani atayekwenda kwa
ajili yetu mbinguni na kutuletea kwetu na kutufanya tuisikie, ili tuweze kutekeleza?”
[13] Wala haipo ng'ambo ya bahari, ili usije ukasema, “Nani atakwenda ng'ambo ya
pili ya bahari kwa ajili yetu na kutuletea kwetu na kutufanya tuisikie, ili tuweze
kuifanya? ”. [14] Lakini neno lipo karibu sana kwako, katika kinywa chako na
moyo wako, ili uweze kutekeleza. [15] Tazama, leo nimeweka mbele yako uzima na
wema, mauti na uovu. [16] Iwapo utatii maagizo ya Yahwe Mungu wako, ambayo
ninakuamuru leo kumpenda Yahwe Mungu wako, kutembea katika njia zake, na
kushikilia amri zake, kanuni zake, na sheria zake, utaishi na kuongezeka, na Yahwe
Mungu wako atakubariki katika nchi ambayo unaingia kumiliki. [17] Lakini moyo wako
ukigeuka, na usisikilize na badala yake unavutwa na kusujudia miungu mingine na
kuwaabudu, [18] basi leo nakutangazia kwako ya kwamba hakika utaangamia; siku
zako hazitaongezeka katika nchi unayoipita juu ya Yordani kuingia na kumiliki.
[19] Naziita mbingu na nchi kushuhudia dhidi yako ya kuwa nimeweka mbele yako
uzima na mauti, baraka na laana; kwa hiyo chagua uzima ili kwamba uweze kuishi,
wewe na uzao wako. [20] Fanya hivi ili umpende Yahwe Mungu wako, kutii sauti yake,

na kung'ang'ania kwake. Kwa maana yeye ni uzima wako na urefu wa siku zako;
fanya hivi ili kwamba uweze kuishi katika nchi ambayo Yahwe aliapa kwa mababu
zako, kwa Abrahamu, kwa Isaka, na kwa Yakobo, kuwapatia.

## 31

1 Musa alikwenda na kuzungumza maneno haya kwa Israeli yote. 2 Alisema kwao,
"Kwa sasa nina umri wa miaka mia moja na ishirini; Siwezi kutoka na kuingia tena;
Yahwe ameniambia, "Hautavuka Yordani hii" 3 Yahwe Mungu wako, atakutangulia
mbele yako; ataangamiza mataifa haya mbele yako, nawe utawanyanganya. Yoshua
atakwenda kabla yako, kama Yahwe alivyonena. 4 Yahwe atawafanya kwao kama
alivyofanya kwa Sihoni na kwa Ogu, wafalme wa Waamori, na kwa nchi yao,
aliyoiangamiza. 5 Yahwe atakupatia ushindi juu yao utakapokutana nao vitani, nawe
utafanya kwao yote ntakayokuamuru. 6 Uwe hodari na mwenye ujasiri mwema,
usiogope, na usiwaogope; kwa maana Yahwe Mungu wako, ni yeye aendaye kabla
yako; hatakuangusha wala kukuacha." 7 Musa akamwita Yoshua na akamwambia
machoni pa Israeli yote, "Uwe hodari na mwenye ujasiri mwema, kwa kuwa
utaondoka na hawa watu katika nchi ambayo Yahwe ameapa kwa mababu zao
kuwapatia; utafanya wairithi. 8 Yahwe, yeye ndiye atakwenda kabla yako; atakuwa
pamoja nawe; hatakuangusha wala hatakutelekeza; usiogope, usivunjike moyo."
9 Musa aliandika sheria hii na kuwapatia makuhani, wana wa Walawi, ambao
walibeba sanduku la agano la Yahwe; pia aligawa nakala zake kwa wazee wote
wa Israeli. 10 Musa aliwaamuru na kusema, "Katika kila mwisho wa miaka saba,
kwa muda uliowekwa wa kudumu kwa ajili ya kufuta madeni, katika Sikukuu ya
Vibanda, 11 ambapo Israeli yote imekuja kujitokeza mbele ya Yahwe Mungu wako
katika mahali atakayochagua kuwa patakatifu pake, utasoma sheria hii mbele ya
Israeli yote wakisikia. 12 Kusanya watu, wanaume, wanawake, na wadogo, na
mgeni wako aliye miongoni mwa malango yako, ili waweze kusikia na kujifunza,
na ili kwamba wamheshimu Yahwe Mungu wako na kushika maneno yote ya sheria
hii. 13 Fanya hivi ili kwamba watoto wao, ambao hawajajua, waweze kusikia na
kujifunza kumheshimu Yahwe Mungu wako, maadamu unaishi katika nchi ambayo
utaenda juu ya Yordani kuimiliki." 14 Yahwe alimwambia Musa, "Tazama, siku
inakuja ambayo lazima utakakufa; muite Yoshua na mjidhihirishe katika hema la
makutano, ili kwamba niweze kuwapatia amri. " Musa an Yoshua waliondoka na
kujidhihirisha katika hema la makutano. 15 Yahwe alijifunua kwenye hema kwa
nguzo ya wingu; nguzo ya wingu ilisimama juu ya mlango wa hema. 16 Yahwe
alimwambia Musa, "Tazama, utalala na baba zako; watu hawa watainuka na
kujifanya kama kahaba na kwenda kwa miungu ya ajabu ambayo imo miongoni
mwao katika nchi wanapokwenda. Wataniacha na kuvunja agano langu ambalo
nimefanya nao. 17 Basi, katika siku hiyo, hasira yangu itawaka dhidi yao nami
nitawaacha. Nitaficha uso wangu kwao nao watamezwa. Maafa na taabu nyingi
yatawakumba ili waseme katika siku hiyo, "Maafa haya hayajaja kwetu kwa sababu
Mungu hayupo kati yetu? " 18 Hakika nitaficha uso wangu kwao katika siku hiyo
kwa sababu ya uovu wote ambao watakuwa wametenda, kwa sababu wamegeukia
miungu mingine. 19 Basi sasa andika wimbo huu kwa ajili yenu na wafundishe watu
wa Israeli. Uweke vinywani mwao, ili kwamba wimbo huu uweze kuwa shahidi
kwangu dhidi ya watu wa Israeli. 20 Kwa maana nitakapowaleta katika nchi ambayo
niliapa kwa mababu zao, nchi inayotiririka kwa maziwa na asali, na watakapokula
na kuridhika na kunenepa, ndipo watageukia miungu mingine nao watawatumikia
na kunidharau na watavunja agano langu. 21 Maovu na taabu nyingi zitakapokuja
juu ya watu hawa, huu wimbo utashuhudia mbele yao (kwa maana hautasahaulika

vinywani mwa uzao wao). Kwa maana najua mipango wanayotengeneza leo, hata
kabla sijawaleta katika nchi niliyowaahidi. 22 Kwa hiyo Musa aliandika huu wimbo
siku hiyo hiyo na kuwafundisha watu wa Israeli. 23 Yahwe alimpa Yoshua mwana
wa Nuni amri na kusema, "Uwe hodari na mwenye ujasiri mwema; kwa maana
utawaleta watu wa Israeli katika nchi niliyoapa kwao, nami nitakuwa pamoja nawe."
24 Ikatokea kwamba Musa alipomaliza kuandika maneno ya sheria hii katika kitabu,
25 aliwaamuru Walawi waliobeba sanduku la agano la Yahwe, na kusema, 26 "Chukua
kitabu hiki cha sheria na kiweke pembeni mwa sanduku la agano la Yahwe Mungu
wenu, ili kiweze kuwa pale kama ushahidi dhidi yenu. 27 Maana nafahamu uasi wenu
na shingo zenu ngumu; tazama, maadamu nipo hai pamoja nanyi hata leo, mmekuwa
waasi dhidi ya Yahwe; itakuaje baada ya mimi kufa? 28 Nikusanyieni wazee wote
wa makabila yenu, na maafisa wenu, ili nizungumze maneno haya masikioni mwao
na kuziita mbingu na nchi kushuhudia dhidi yao. 29 Kwa maana najua baada ya
kifo changu mtajiharibu kabisa na kugeuka kuiacha njia niliyowaamuru; maafa
yatawakumba katika siku zijazo. Haya yatatokea kwa sababu mtafanya yaliyo maovu
machoni pa Yahwe, ili kumchokoza katika hasira kwa mikono ya kazi yenu." 30 Musa
alinena masikioni mwa kusanyiko lote la Israeli maneno yote ya wimbo huu hadi
yalipokamilika.

# 32

1 Tega sikio, enyi mbingu, na niruhusu kuzungumza. 2 Acha dunia isikie maneno
ya kinywa changu. Acha mafundisho yangu yamwagike chini kama mvua, acha
usemi wangu udondoke kama umande, kama mvua tulivu juu ya majani laini,
na kama mvua za manyunyu juu ya mimea. 3 Kwa maana nitatangaza jina la
Yahwe, na kumpatia ukuu Mungu wetu. 4 Mwamba, kazi yake ni kamili; kwa
maana njia zake ni za haki. Yeye ni Mungu mwaminifu, hana udhalimu. Yeye ni
wa haki na mwadilifu. 5 Wamefanya yaliyo maovu dhidi yake. Wao sio watoto
wake. Ni aibu kwao. Wao ni kizazi kiovu na kilichopindika. 6 Je! Unamzawadia
Yahwe kwa njia hii, enyi watu wapumbavu na msiojitambua? Je! yeye si baba
yenu, yule ambaye aliwaumba? Aliwaumba na kuwaimarisha. 7 Kumbukeni siku
zile za zamani, tafakari juu ya miaka mingi ya nyuma. Muulize baba yako naye
atakuonyesha, wazee wako nao watakuambia. 8 Pale ambapo Aliye Juu alipowapatia
mataifa urithi wao – alipowagawa wanadamu wote, na kuweka mipaka ya watu, na
alipoimarisha idadi ya miungu yao. 9 Kwa maana fungu la Yahwe ni watu wake;
Yakobo ni mgao wa urithi wake. 10 Alimpata katika nchi ya jangwa, na katika
jangwa kame na livumalo upepo; alimkinga na kumtunza, alimlinda kama mboni
ya jicho lake. 11 Kama tai akichungaye kiota chake na kupiga piga mabawa juu
ya makinda yake, Yahwe alitandaza mabawa yake na kuwachukua, na kuwabeba
kwenye mapapatio yake. 12 Yahwe pekee alimuongoza, hapakuwa na mungu mgeni
pamoja naye. 13 Alimfanya aendeshe katika maeneo ya juu ya nchi, na alimlisha
matunda ya mbugani; alimrutubisha kwa asali kutoka kwenye jiwe, na mafuta kutoka
kwenye mwamba mgumu sana. 14 Alikula siagi kutoka katika kundi na kunywa
maziwa kutoka katika kundi la mifugo, pamoja na mafuta ya wanakondoo, kondoo
dume wa Bashani na mbuzi, pamoja na ngano safi kabisa – nawe ulikunywa divai
itokayo povu iliyotengenezwa kwa juisi ya mizabibu. 15 Lakini Yeshuruni akakua
kwa unene na kupiga mateke – ulikua kwa unene, ulikua mnene sana, na ulikuwa
umekula ujazo wako – alimuacha Mungu aliyemuumba, na kukataa Mwamba wa
wokovu wake. 16 Walimfanya Yahwe apatwe wivu kwa miungu yao ya ajabu; kwa
maudhi yao walimkasirisha. 17 Walitoa dhabihu kwa mapepo, ambayo sio Mungu
– miungu ambayo hawajaijua, miungu ambayo imejitokeza hivi karibuni, miungu

ambayo mababu zenu hawakuogopa. 18 Umetelekeza Mwamba, ambao ulikuwa baba
yako, na ukasahau Mungu aliyekuzaa. 19 Yahwe aliliona hili na kuwakataa, kwa
sababu watoto wake wa kiume na mabinti zake walimchokoza. 20 "Nitaficha uso
wangu kwao", alisema, "nami nitaona mwisho wao utakuaje; maana wao ni kazazi
kaidi, watoto ambao sio waaminifu. 21 Wamenifanya kuwa na wivu kwa kile ambacho
sio mungu na kunikasirisha kwa mambo yao yasiyo na maana. Nitawafanya waone
wivu kwa wale ambao sio taifa; nitawakasirisha kwa taifa pumbavu. 22 Kwa maana
moto kuwashwa kwa hasira yangu na inawaka hadi chini mwa Sheoli; inameza
ulimwengu na mavuno yake; inawasha moto misingi ya milima. 23 Nitarundia maafa
juu yao; nitafyatua mishale yangu yote kwao; 24 Watapotea kwa njaa na kumezwa
kwa joto liwakalo na uharibifu mchungu; nitatuma kwao meno ya wanyama wa
mwituni, pamoja na sumu ya vitu vitambaao mavumbini. 25 Nje panga litawatwaa,
na ndani ya vyumba hofu kuu itafanya hivyo. Wote mwanamume kijana na bikra
nitawaangamiza, mchanga anyonyaye, na mwanamume mwenye mvi. 26 Nilisema
nitawasambaza mbali, kwamba nitafanya kumbukumbu yao kukoma miongoni mwa
wanadamu. 27 Isingekuwa kwamba naogopa uchokozi wa adui, na kwamba adui
zake wangehukumu kimakosa, na kwamba wangesema, "Mkono wetu umeinuliwa, "
ningefanya haya yote. 28 Kwa maana Israeli ni taifa linalopungukiwa na hekima, na
hakuna ufahamu ndani mwao. 29 Ah laiti wangekuwa na hekima, wangeelewa hili,
na kuzingatia ujio wa hatima yao! 30 Inawezekanaje mmoja kufukuza maelfu, na
wawili kuweka makumi elfu mbioni, isipokuwa Mwamba wao hajawauza, na Yahwe
hajawaachilia kwao? 31 Kwa maana mwamba wa maadui zetu si kama Mwamba
wetu, kama vile maadui zetu wanavyokiri. 32 Kwa maana mzabibu wao unatoka
kwenye mzabibu wa Sodoma, na kwenye mashamba ya Gomorra; na zabibu zake ni
zabibu za sumu; vishada vyao ni vichungu. 33 Mvinyo yao ni sumu ya nyoka na sumu
katili ya nyoka. 34 Huu mpango haujafichwa kwangu kwa siri, na kufungwa kabisa
katika hazina zangu? 35 Kisasi ni changu kutoa, na fidia, katika muda mguu wao
utakapotereza; kwa maana siku ya maafa kwao ipo karibu, na vitu vitakavyokuja
juu yao vitaharakisha kutendeka. 36 Kwa maana Yahwe atatoa haki kwa watu wake,
na atawahurumia watumishi wake. Atahakikisha kuwa nguvu yao imetoweka, na
hakuna atakayesalia, iwe watumwa au watu huru. 37 Kisha atasema, "wako wapi
miungu yao, mwamba ambao wamekimbilia? – 38 miungu iliyokula sadaka zao nene
na kunywa mvinyo wa sadaka zao za kinywaji? Na wainuke na kukusaidia; na wawe
ulinzi kwako. 39 Tazama sasa mimi, hata mimi, ni Mungu, na kwamba hakuna mungu
tofauti yangu; ninaua, na ninaleta uhai; ninajeruhi, na ninaponya, na hakuna mtu
atakayekuokoa kutoka kwa uwezo wangu. 40 Kwa maana ninainua mikono yangu
mbinguni na kusema, "Niishivyo milele, nitatenda. 41 Nitakapong'oa panga langu
lingaaro, na mkono wangu utakapoanza kuleta haki, nitalipiza kisasi juu ya maadui
zangu, na kuwalipa wale wote wanichukiao. 42 Nitafanya mishale yangu kulewa na
damu, na panga langu litameza nyama kwa damu ya waliouawa na mateka, na kutoka
kwa vichwa vya viongozi wa adui." 43 Furahi, enyi mataifa, na watu wa Mungu,
kwa maana atalipiza kisasi damu ya watumishi wake; atalipiza kisasi juu ya maadui
zake, naye atafanya upatanisho kwa ajili ya nchi yake, kwa watu wake. 44 Musa
alikuja na kunena maneno yote ya wimbo huu masikioni mwa watu, yeye na Yoshua
mwana wa Nuni. 45 Kisha Musa alimaliza kunena maneno haya yote kwa Israeli yote.
46 Aliwaambia, "Imarisheni akili yenu kwa haya maneno ambayo nimewashuhudia
kwenu leo, ili kwamba muwaamuru watoto wenu kuyashika, maneno yote ya sheria
hii. 47 Kwa maana hili si jambo dogo kwako, kwa sababu ni uzima wako, na kupitia
jambo hili utarefusha siku zako katika nchi ambayo unakwenda juu ya Yordani
kumiliki." 48 Yahwe alizungumza na Musa katika siku hiyo hiyo na kusema, 49 "Nenda

katika usawa huu wa milima wa Abarimu, juu ya mlima wa Nebo, ambao upo
katika nchi ya Moabu, mkabala na Yeriko. Utatazama nchi ya Kanani, ambayo
ninawapatia watu wa Israeli kama miliki yao. 50 Utakufa katika mlima utakaopanda,
na utakusanywa kwa watu wako, kama Haruni Muisraeli mwenzako alivyokufa juu
ya mlima wa Hori na kukusanywa kwa watu wake. Hii 51 itatendeka kwa sababu
haukuwa mwaminifu kwangu miongoni mwa watu wa Israeli katika maji ya Meriba
kule Kadeshi, katika jangwa la Zini; kwa sababu haukunitendea utukufu na heshima
miongoni mwa watu wa Israeli. 52 Kwa maana utaona nchi mbele yako, lakini
hautakwenda kule, katika nchi ninayowapatia watu wa Israeli."

# 33

1 Hii ni baraka ambayo Musa mtu wa Mungu aliwabariki watu wa Israeli kabla ya
kifo chake. 2 Alisema: Yahwe alikuja kutoka Sinai na akainuka kutoka Seiri juu yao.
Aling'ara kutoka mlima wa Paramu, na akaja na elfu kumi ya watakatifu. Katika
mkono wake wa kuume radi zilimulika. 3 Kweli, anawapenda watu; watakatifu wake
wote wapo mikononi mwako, na walimsujudu mguuni mwake; walipokea maneno
yako. 4 Musa alituamuru sheria, urithi kwa kusanyiko la Yakobo. 5 Kisha pakawa
na mfalme Yeshurumu, pale ambapo wakuu wa watu walipokusanyika, makabila
yote ya Israeli pamoja. 6 Acha Rubeni aishi na asife, lakini wanaume wake wawe
wachache. 7 Hii ni baraka ya Yuda. Musa akasema: Sikiliza sauti ya Yuda, Yahwe,
na umlete kwa watu wake tena. Mpiganie; kuwa msaada dhidi ya maadui wake.
8 Kuhusu Lawi, Musa akasema: Thumimu yako na Urimu yako ni ya mtakatifu wako,
yule uliyemjaribu kule Masa, ambaye ulishindana naye katika maji ya Meriba. 9 Mtu
aliyesema juu ya baba na mama yake, "Sijawaona. " Wala hakuwatambua kaka zake,
wala hakuzingatia juu ya watoto wake wenyewe. Kwa maana alilinda neno lako na
kushika agano lako. 10 Anafundisha Yakobo maagizo yako na Israeli sheria yako.
Ataweka ubani mbele yako na sadaka kamili ya kuteketezwa juu ya dhabahu lako.
11 Bariki mali zake, Yahwe, na kubali kazi ya mikono yake. Vunja viuno vya wale
wanaoinuka dhidi yake, na wale watu wanaomchukia, ili wasiinuke tena. 12 Kuhusu
Benyamini, Musa akasema: Yule anayependwa na Yahwe anaishi kwa usalama kando
yake; Yahwe anamkinga siku nzima, naye huishi katikati ya mikono ya Yahwe.
13 Kuhusu Yusufu, Musa akasema: Nchi yake na ibarikiwe na Yahwe na vitu vya
thamani vya mbinguni, na umande, na kina kilalacho chini. 14 Nchi yake na ibarikiwe
na vitu vya thamani mavuno ya jua, na vitu vya thamani mazao ya miezi, 15 kwa
vitu vizuri vya milima ya zamani, na kwa vitu vya thamani vya milima ya milele.
16 Nchi yake ibarikiwe na vitu vya thamani vya ardhi na wingi wake, na kwa mapenzi
mema ya yule aliyekuwa kichakani. Baraka na ifike juu ya kichwa cha Yusufu, na
juu ya kichwa cha yule aliyekuwa mwana wa mfalme kwa kaka zake. 17 Mzawa wa
kwanza wa ng'ombe, katika utukufu wake, na pembe zake ni pembe za ng'ombe
mwitu. Kwa hawa atawasukuma watu, wote, hadi mwisho wa ulimwengu. Hawa
ni maelfu makumi ya Efraimu; hawa ni maelfu wa Manase. 18 Kuhusu Zabuloni,
Musa alisema: Furahi, Zabuloni, katika kutoka kwako, na wewe, Isakari, katika
mahema yako. 19 Watawaita watu hadi milimani. Huko watatoa sadaka za utakatifu.
Maana watanyonya wingi wa bahari, na mchanga wa ufukweni. 20 Kuhusu Gadi,
Musa alisema: Abarikiwe yule amkuzaye Gadi. Ataishi pale kama simba jike, naye
atanyakua mkono au kichwa. 21 Alitoa sehemu nzuri kwake mwenyewe, maana
kulikuwa na fungu la ardhi la kiongozi lililohifadhiwa. Alikuja na vichwa vya watu.
Alitekeleza haki ya Yahwe na maagizo yake pamoja na Israeli. 22 Kuhusu Dani, Musa
alisema: Dani ni mwana wa simba arukaye kutoka Bashani. 23 Kuhusu Naftali, Musa
alisema: Naftali, aliyeridhika na fadhila, na kujaa kwa baraka za Yahwe, miliki nchi

iliyopo magharibi na kusini. [24] Kuhusu Asheri, Musa alisema: Abarakiwe Asheri Zaidi
ya watoto wengine wa kiume; naye akubalike kwa kaka zake, na achovye mguu wake
ndani ya mafuta ya zeituni. [25] Vyuma vya mji wako na viwe chuma na shaba; kama
vile siku zako zitakavyokuwa, ndivyo usalama wako utakavyokuwa. [26] Hakuna aliye
kama Mungu, Yeshurumu – aliyekamili, anayeendesha katika mbingu kukusaidia, na
katika utukufu wake juu ya mawingu. [27] Mungu wa milele ni kimbilio, na chini yake
kuna mikono ya milele. Husukuma adui mbele yako, naye alisema, “Angamiza!”
[28] Israeli waliishi katika usalama. Wana wa Yakobo walikuwa salama katika nchi ya
nafaka na divai mpya; hakika, mbingu na idondoshe umande juu yake. [29] Baraka
zako ni nyingi, Israeli! Nani kama wewe, watu waliokombolewa na Yahwe, ngao
ya msaada wako, na upanga wa utukufu wako? Maadui zako watakuja kwako kwa
kutetemeka; utakanyanga sehemu zao zilizoinuka.

# 34

[1] Musa aliondoka kutoka nyanda za Moabu mpaka mlima wa Nebo, hadi kilele cha
Pisga, kilicho mkabala na Yericho. Huko Yahwe alimwonyesha nchi yote ya Gileadi
kutoka umbali wa Dani, [2] na Naftali yote, na nchi ya Efraimu na Manase, na nchi
yote ya Yuda, mpaka bahari ya magharibi, [3] na Negevi, na uwanda wa bonde la
Yericho, mji wa mitende, mpaka umbali wa Soari. [4] Yahwe alimwambia, “Hii ni nchi
niliyoapa kwa Abrahamu, kwa Isaka, na kwa Yakobo, na kusema, “Nitawapatia uzao
wako. ” Nimekuruhusu uitazame kwa macho yako, lakini hautakwenda kule. ”
[5] Basi Musa mtumishi wa Yahwe, alikufa pale katika nchi ya Moabu, kama neno la
Yahwe lilivyoahidi. [6] Yahwe alimzika katika bonde katika nchi ya Moabu mkabala na
Beth-peori, lakini hakuna ajuaye kaburi lake lilipo hadi leo hii. [7] Musa alikuwa na
umri wa miaka mia moja na ishirini alipokufa; macho yake hayakufifia, wala nguvu
asili zake hazikupungua. [8] Watu wa Israeli walimuomboleza Musa katika nyanda
za Moabu kwa siku thelathini, hapo ndipo siku za maombolezo ya Musa zilipotimia.
[9] Yoshua mwana wa Nuni alikuwa amejawa na roho ya hekima, kwa maana Musa
alimwekea mkono juu yake. Watu wa Israeli walimsikiliza na kufanya yale ambayo
Yahwe alimuamuru Musa. [10] Tangu hapo hakujatokea nabii katika Israeli kama Musa,
ambaye Yahwe alimjua uso kwa uso. [11] Hakujawahi kuwa na nabii yeyote kama yeye
kwa ishara na miujiza ambayo Yahwe alimtuma kufanya katika nchi ya Misri, kwa
Farao, na kwa watumishi wake, na kwa nchi yake yote. [12] Hakujawahi kuwa na nabii
yeyote kama yeye kwa mambo yote makubwa, ya kutisha ambayo Musa aliyafanya
machoni pa Israeli yote.

# Yoshua

[1] Sasa ilitokea baada ya kufa kwa Musa, mtumishi wa Yahweh, Yahweh alimwambia
Yoshua, mwana wa Nuni, msaidizi mkuu wa Musa, kusema, [2] “Musa, mtumishi
wangu amekufa. Sasa basi inuka, vuka mto huu wa Yordani, wewe na watu hawa
wote, kuingia katika nchi ambayo ninawapa - watu waisraeli. [3] Nimewapa ninyi
kila sehemu ambapo nyayo za miguu yenu itakanyaga. Nimewapa ninyi, kama
nilivyomwahidi Musa. [4] kuanzia jangwani na Lebanoni, hadi mto mkubwa wa Frati,
nchi yote ya Wahiti, na hata Bahari kuu, ambako jua huzama, itakuwa nchi yenu.
[5] Hakuna mtu awaye yote atakayeweza kusimama kinyume chako siku zote za maisha
yako. Nitakuwa pamoja nawe kama nilivyokuwa na Musa. Sitakupungukia wala
kukuacha. [6] Uwe hodari na jasiri. Wewe utawafanya watu hawa wairithi nchi
ambayo niliwaahidi baba zao kuwa ningewapa. [7] Uwe hodari na jasiri sana. uwe
makini kutii sheria zote ambazo Musa mtumishi wangu alikuagiza. Usikengeuke
upande wa kulia au wa kushoto, ili uweze kufanikiwa kila mahali utakapoenda. [8] Siku
zote uuongee juu ya kitabu hiki cha sheria. Utakitafakari mchana na usiku ili kwamba
uweze kutii yote yaliyoandikwa humo. Kisha utastawi na kufanikiwa. [9] Je si mimi
niliyekuagiza? Uwe hadori na jasiri! Usiogope. Usivunjike moyo. Yahweh Mungu
wako yuko pamoja nawe kila uendeko. [10] Kisha Yoshua akawaagiza viongozi wa
watu, [11] “Nendeni katika kambi na waagizeni watu, 'andaeni chakula kwa ajili yenu.
Baada ya siku tatu mtavuka mto huu wa Yordani na kuingia ndani na kuimiliki nchi
ambayo Yahweh Mungu wenu awapeni ninyi ili kuimiliki.”” [12] Yoshua akawaambia
Wareubeni, Wagadi na nusu ya kabila la Manase, [13] “Kumbukeni maneno ambayo
Musa, mtumishi wa Yahweh, aliwaaagiza aliposema, 'Yahweh Mungu wenu awapeni
ninyi pumziko, naye awapeni ninyi nchi hii.' [14] Wake zenu, na watoto wenu na mifugo
yenu itakaa katika nchi ambayo Musa aliwapa ninyi ng'ambo ya Yordani. Lakini watu
wenu wa vita wataenda pamoja na ndugu zao na kuwasaidia. [15] Mpaka hapo Yahweh
atakapowapa ndugu zenu pumziko kama alivyowapa ninyi. Na wao pia watamiliki
nchi ambayo Yahweh Mungu wenu awapeni ninyi. Kisha mtarudi katika nchi yenu
na kuimiliki, nchi ambayo Musa mtumishi wa Yahweh aliwapa ninyi ng'ambo ya
Yordani, mahali pa mapambazuko ya jua.” [16] Nao wakamjibu Yoshua, na kusema,
“ Mambo yote uliyotuagiza tutayafanya, na kila mahali utakapotutuma tutaenda.
[17] Tutakutii kama tulivyomtii Musa. Yahweh Mungu wako na awe pamoja nawe
tu kama aliyokuwa pamoja na Musa. [18] Yeyote anayeasi maagizo yako na kutotii
maneno yako atauawa. Uwe hodari na jasiri tu.

## 2

[1] Kisha Yoshua mwana wa Nuni aliwatuma watu wawili kwa siri kama wapelelezi
kutoka Shitimu. Akisema, “Nendeni mkaiangalie nchi, hasa Yeriko.” Walienda na
wakafika katika nyumba ya kahaba ambaye jina lake ni Rahabu, na wakalala hapo.
[2] Mfalme wa Yeriko aliambiwa, “Tazama watu wa Israeli wamekuja kuipeleleza nchi.”
[3] Mfalme akatuma neno kwa Rahabu kusema, “ Watoe watu waliokuja kwako ambao
wameingia nyumbani mwako, kwa kuwa wamekuja kuipeleleza nchi yote.” [4] Lakini
mwanamke alikuwa amekwisha kuwachukua wale watu wawili na kuwaficha. Na
akasema, “Ndiyo, watu walikuja kwangu, lakini sikujua walikotoka. [5] Ilipokuwa
jioni wakati wa kufungwa kwa lango la mji, waliondoka. Sijui mahali walikoelekea.
Mnaweza kuwakamata kama mtawafuata upesi. [6] Lakini yeye aliwapandisha juu
darini na kuwaficha kwa mabua ya kitani ambayo alikuwa ameyalaza darini.

7 Hivyo, watu waliwafuatilia njiani iliyoeleka katika vivuko vya Yordani. Na milango
ilifungwa mara tu baada ya wale watu waliofuata kutoka nje. 8 Wale wanaume
walikuwa hajalala usiku, wakati alipowaendea kule darini. 9 Akawaambia, " Ninajua
kwamba Yahweh amewapa ninyi nchi na kwamba hofu juu yenu imetuingia. Watu
wote wanaoishi katika nchi watayeyuka mbele yenu. 10 Tumesikia jinsi ambavyo
Yahweh alivyokausha maji ya Bahari ya Mianzi kwa ajili yenu wakati mkitoka
Misri. Na tumesikia mlichokifanya kwa wafalme wawili wa Waamori walioko
upande mwingine wa Yordani - Sihoni na Ogu - ambao mmewaangamiza kabisa.
11 Mara tu tuliposikia, mioyo yetu iliyeyuka na hapakuwa na ujasiri wowote uliosalia
kwa mtu yeyote - kwa kuwa Yahweh Mungu wenu, ni Mungu aliye juu mbinguni
na chini duniani. 12 Sasa basi, tafadhali mniapie kwa Yahweh kwamba kama
nilivyokuwa mwema kweu, nanyi pia mtaitendea mema nyumba ya baba yangu.
Nipeni ishara ya uhakika 13 kwamba mtanihifadhi maisha ya baba, mama, kaka,
dada zangu na famiie zao, na kwamba mtatuokoa kutoka katika kifo. 14 Wanaume
wakamjibu, "maisha yetu kwa ajili ya yenu, hata kifo! Kama hamtasema habari
zetu, na Yahweh akisha kutupa nchi hii, tutakuwa wenye huruma na waaminifu
kwenu." 15 hivyo aliwashusha chini kwa kupitia dirishani kwa kutumia kamba.
Nyumba ambayo alikuwa anaishi ilijengwa katika ukuta wa mji. 16 Akawaambia,
"Nendeni milimani la sivyo watu waliowafuata watawaona. Jificheni huko kwa siku
tatu mpaka watu waliowafuata watakaporudi. Kisha nendeni zenu." 17 Wanaume
wakamwambia, "Hatutakuwa tumefungwa na ahadi ulizotufanya tuape mbele zako,
kama hautalifanya hili. 18 Tutakapokuja katika nchi, ni lazima uifunge kamba hii
nyekundu katika dirisha ulilotushushia chini, na utawakusanya katika nyumba baba
yako, mama yako, kaka zako na wote wa nyumba ya baba yako. 19 Na yeyote aendaye
mtaani nje ya milango ya nyumba yako,, damu yao itakuwa juu ya vichwa vyao na
hatutakuwa na hatia yoyote. Lakini kama mkono utanyoshwa juu ya mtu yeyote aliye
pamoja nawe katika nyumba, damu yake itakuwa juu ya vichwa vyetu. 20 Na ikiwa
utaongea juu ya suala letu, tutakuwa huru dhidi ya kiapo ulichotuapisha. 21 Rahabu
akawajibu, " Yote mliyosema nayatimie." Akawatoa mbali na wakaondoka. Kisha
akaifunga kamba nyekundu katika dirisha. 22 Wakaondoka na kwenda juu milimani
na walikaa huko kwa siku tatu hadi pale wale waliowafuatilia waliporudi. Wale
waliowafuata walitafuta njiani pote bila kuwaona. 23 Wale watu wawili walirudi na
kuvuka mto na wakafika kwa Yoshua mwana wa Nuni, na walimwambia kila kitu
kilichotokea kwao. 24 Nao wakasema kwa Joshua, "kwa kweli Yahweh ametupa nchi
hii. Wenyeji wote wa nchi wanayeyuka kwasababu yetu.

# 3

1 Yoshua aliamka asubuhi na mapema, nao walisafiri kutoka Shitimu. Walifika
Yordani, yeye na watu wote wa Israeli, na wakapiga kambi hapo kabla hawajavuka
ng'ambo. 2 Baada ya siku tatu, maafisa walienda katika kambi, wakawaagiza
watu, 3 "Mtakapoona sanduku la agano la Yahweh Mungu wenu, na makuhani
kutoka miongoni mwa Walawi wamelibeba, ni lazima muondoke sehemu hii na
kulifuata. 4 Lazima kuwe na umbali wa dhiraa elfu moja kati yenu na sanduku.
Msilisogelee karibu, ili muweze kuiona njia ya kupitia, kwakuwa hamjawahi kupita
njia hii kabla. 5 Yoshua akawaambia watu, "Jitakaseni ninyi wenyewe keso, kwa
kuwa Yahweh atafanya maajabu miongoni mwenu." 6 Kisha Yoshua akawaambia
makuhani, "Chukueni sanduku la agano, na kulipitisha mbele za watu." Hivyo,
wakalichukua sanduku la agano na wakaenda mbele za watu. 7 Yahweh akamwambia
Yoshua, "Siku hii nitakufanya kuwa mtu mkubwa katika macho ya Waisraeli wote.
Watajua kuwa kama nilivyokuwa na Musa ndivyo nitakavyokuwa pamoja na wewe.

8 Utawaamuru makuhani ambao hulibeba sanduku la agano, 'Mtakapofika katika
ukingo wa maji ya Yordani, ni lazima msimame katika Mto Yordani.'” 9 Kisha
Yoshu akawaambia watu wa Israeli, “Njooni hapa na msikilize maneno ya Yahweh
Mungu wenu. 10 Kwa hili mtajua kwamba Mungu aliye hai yuko miongoni mwenu
na kwamba atawaondosha mbele yenu Wakanaani, Wahiti, Wahivi, Waperizi,
Wagrigashi, Waamori na Wayebusi. 11 Tazama! Sanduku la agano la Bwana wa
nchi yote litavuka mbele yenu katika Yordani. 12 Sasa chagueni wanaume kumi
na wawili kutoka katika makabila ya Israeli, mmoja katika kila kabila. 13 Wakati
nyayo za miguu ya makuhani walichukualo sanduku la Yahweh, Bwana wa nchi yote,
zitakapogusa maji ya Yordani, maji ya Yordani yatatindika, na hata maji yatiririkayo
kutoka juu yatakoma kutiririka nayo yatasimama kama chuguu. 14 Hivyo wakati watu
walipotoka ili kuvuka Yordani, makuhani waliobeba sanduku la agano waende mbele
ya watu. 15 Mara tu wale walichukuao sanduku wakiisha kufika Yordani, na miguu
ya watu wale waliobeba sanduku itakapotiwa katika ukingo wa maji (maana sasa
Yordani hujaa hadi katika kingo zake zote katika kipindi chote cha mavuno), 16 maji
yote yaliyotiririka kutoka juu yalisimama katika chuguu kimoja. Maji yakakoma
kutiririka kutoka katika umbali mrefu. Maji yaliacha kutiririka kutoka Adam, mji
ulio karibu na Zarethani, hadi bahari ya Negevu, Bahari ya Chumvi. Na watu
walivuka ng'ambo karibu na Yeriko. 17 Makuhani waliolibeba sanduku la agano la
Yahweh walisimama katika nchi kavu katikati ya Yordani mpaka watu wote wa Israeli
walipokwisha kuvuka katika nchi kavu.

# 4

1 Watu wote walipokwisha kuvuka Yordani, Yahweh akamwambia Yoshua,
2 “Chagueni wenyewe watu waume kumi na wawili, mmoja katika kila kabila.
3 Wape agizo hilo: 'Chukueni mawe kumi na mbili kutoka katikati ya Yordani mahali
wanaposimama makuhani katika nchi kavu, na wayalete na kuyaweka chini katika
sehemu ambapo mtalala usiku wa leo. 4 Kisha Yoshua akawaita wanaume kumi
na wawili ambao aliwachagua kutoka katika makabila ya Israeli, mmoja kutoka
kila kabila. 5 Yoshua akawaambia, “Nendeni mbele za sanduku la Yahweh Mungu
wenu katikati ya Yordani. Kila mmoja wenu achukue jiwe moja mabegani mwake,
kulingana na hesabu ya makabila ya watu wa Israeli. 6 Hii itakuwa ni ishara
miongoni mwenu kwa ajili yenu wakati watoto wenu watakapowauliza katika siku
zijazo, 'Nini maana ya mawe haya kwenu?' 7 Ndipo mtakapowaambia, 'Maji ya
Yordani yalitengwa mbele ya sanduku la Yahweh. Lililpopitishwa katika Yordani,
maji ya Yordani yalisimamishwa. Hivyo, mawe haya yatakuwa kumbukumbu kwa
watu wa Israeli milele.'” 8 Watu waisraeli walifanya kama Yoshua alivyowaagiza,
na walichukua mawe kumi na mbili kutoka katikati ya Yordani, kama Yahweh
alivyomwambia Yoshua, walipangwa sawa sawa na hesabu ya makabila ya watu
wa Israeli. Waliyachukua mawe mpaka mahali walipolala na wakayaweka chini
huko. 9 Kisha Yoshua akayapanga mawe kumi na mbili katikati ya Yordani, katika
sehemu ambapo ilisimama miguu ya makuhani waliolichukua sanduku la agano. Na
kumbukumbu hiyo ipo hadi leo. 10 Makuhani waliolichukua sanduku walisimama
katikati ya Yordani mpaka pale kila kitu ambacho Yahweh alimwamuru Yoshua
kuwaambia watu kilipokamilika, sawa sawa na yote ambayo Musa alimwagiza
Yoshua. Watu walifanya haraka na wakavuka. 11 Wakati watu wote walipokwisha
kuvuka, sanduku la Yahweh pamoja na makuhani walivuka mbele za watu. 12 Kabila
la Rubeni, kabila la Gadi, na nusu ya kabila la Manase walipita kama jeshi mbele
ya watu wa Israeli, kama ambavyo Musa alivyowaambia. 13 Yapata watu watu
elfu arobaini walioandaliwa kwa vita walipita mbele za Yahweh, kwa ajili ya vita

katika uwanda wa Yeriko. 14 Katika siku hiyo Yahweh alimfanya Yoshua kuwa mkuu
katika macho ya watu wote wa Israeli. Walimheshimu - kama walivyomheshimu
Musa - siku zake zote. 15 Kisha Yahweh akamwambia Yoshua, 16 “Waamuru
makuhani wanaolibeba sanduku la ushuhuda watoke katika Yordani.” 17 Hivyo
Yoshua akawaamuru makuhani, '' pandeni mtoke Yordani.” 18 Wakati makuhani
wenye kulibeba sanduku la agano la Yahweh walitoka katikati ya Yordani, na
nyayo za miguu yao ilikuwa imeinuliwa katika nchi kavu, kisha maji ya Yordani
yalirudi katika sehemu zake na kujaa hadi katika kingo zake kama ilivyokuwa
siku nne zilizopita. 19 Katika siku ya kumi ya mwezi wa kwanza, watu walikwea
kutoka Yordani. Wakakaa huko Gilgali, mashariki mwa Yeriko. 20 Mawe kumi na
mawili ambayo yalichukuliwa katika Yordani, Yoshuua aliyasimamisha hapo Gilgali.
21 Aliwaambia watu wa Israeli, “ wakati watoto wenu watakapowauliza baba zao
katika wakai ujao, 'Mawe haya ni ya nini?' 22 Waambieni watoto wenu, 'Hapa ndipo
Waisraeli walivuka Yordani katika nchi kavu. 23 Yahweh Mungu wenu aliyakausha
maji ya Yordani, mpaka hapo Yahweh Mungu wako aliyoyafanya katika bahari ya
mianzi, ambayo aliikausha kwa ajili yetu ili tupite juu yakes, 24 ili kwamba watu wote
wa nchi wajue kwamba mkono wa Yahweh ni nguvu, na kwamba mtamweshimu
Yahweh Mungu wenu milele.''

# 5

1 Mara tu waliposikia wafalme wa Waamori walio upande wa magharibi wa
Yordani, na wafalme wote wa Wakanaani waliokuwa katika pwani ya Ziwa kuu,
waliposikia ya kwamba Yahweh alikuwa ameyakausha maji ya Yordani mpaka
pale waisraeli wote walipomaliza kuvuka, mioyo yao ikayeyuka, na hapakuwa
na moyo wowote ndani yao kwa sababu ya watu wa Israeli. 2 Kwa wakati huo
Yahweh alimwambia Yoshua, “Tengenezeni visu vya mawe na mara moja mwatahiri
wanaume wote wa Israeli.” 3 Kisha Yoshua alijifanyia visu vya mawe na akawatahiri
wanaume wote wa Gibea Haaraloti. 4 Na hii ndo sababu ya Yoshua kuwatahiri;
wanaume wote waliotoka Misri, pamoja na wanaume wa vita walikuwa wamekwisha
kufa njiani katika nyikani, baada ya kukwea kutoka Misri. 5 Ingawa wanaume
wote waliotoka Misri walikuwa wametahiriwa, bado hapakuwa na kijana yeyote
aliyekuwa ametahiriwa kati ya vijana wote waliozaliwa nyikani katika njia ya
kutoka Misri. 6 Kwasababu watu wa Israeli walitembea nyikani miaka arobaini,
mpaka watu wa vita, yaani wanaume wote waliotoka Misri walikufa, kwasababu
hawakuitii sauti ya Yahweh. Yahweh aliwaapia kwamba hawataruhusu kuiona nchi
ambayo aliwaapia mababa zao kwamba angetupatia sisi, nchi inayotiririka maziwa
na asali. 7 Na badala yao, Yahweh aliwainua watoto wao kuchukua nafasi zao ambao
Yoshua aliwatahiri, kwasababu walikuwa bado hajatahiriwa njiani. 8 Walipokwisha
kutahiriwa wote, walibaki mahali walipokuwa katika kambi mpaka walipopona. 9 Na
Yahweh akasema na Yoshua, “Siku hii nimeiondoa kwenu aibu ya Misri.” Hivyo,
mahali pale paliitwa Gilgali hadi leo. 10 Watu wa Israeli walipiga kambi hapo Gilgali.
Waliitunza Pasaka katika siku ya kumi na nne ya mwezi, wakati wa jioni, katika
uwanda wa Yeriko. 11 Na siku iliyofuata baada ya Pasaka, walikula sehemu ya
mazao ya nchi, mikate isiyotiwa chachu na nafaka iliyokaangwa katika siku hiyo
iyo. 12 Mana zilikoma siku ile walipokula mazao ya nchi. Hapakuwa tena na mana
kwa watu wa Israeli, bali walikula mazao ya nchi ya Kanaani mwaka huo. 13 Wakati
Yoshua alipokaribia Yeriko, aliinua macho na kuangalia, na tazama, mtu alikuwa
amesimama mbele yake, alikuwa amechomoa upanga wake na ulikuwa mkononi
mwake. Yoshua alimwendea na kumwambia, “Je uko kwa ajili yetu au kwa ajli
ya maadui zetu?” 14 Akajibu, la hasha. Maana mimi ni amiri wa jeshi la Yahweh.

Sasa nimekuja. Kisha Yoshua akainamisha uso wake juu ya nchi akaabudu na
akamwambia, “Bwana wangu anasema nini kwa mtumwa wake?” [15] Amiri wa jeshi la
Yahweh akamwambia Musa, “Vua viatu vyako miguuni mwako, kwasababu sehemu
uliyosimama ni takatifu.” Na Yoshua akafanya hivyo.

# 6

[1] Basi, milango yote ya Yeriko ilikuwa imefungwa kwasababu ya jeshi la Israeli.
Hapakuwa na mtu wa kutoka nje au kuingia ndani. [2] Yahweh akamwambia Yoshua,
“Tazama, nimeweka Yeriko katika mkono wako, mfalme wake pamoja na wanajeshi
wake waliofunzwa. [3] Ni lazima kutembea kwa kuuzunguka mji, wanaume wote wa
vita wauzunguke mji mara moja. Ni lazima mfanye hivi kwa siku sita. [4] Makuhani
saba lazima wabebe tarumbeta za pembe za kondoo waume mbele za sanduku.
Na katika siku ya saba, ni lazima mtembee kwa kuuzunguka mji mara saba, na
makuhani lazima wapulize tarumbeta. [5] Kisha watapuliza pembe za kondoo waume
kwa nguvu kuu, na mtakaposikia sauti za tarumbeta watu wote na wapige kelele
kwa mshindo mkuu, na ukuta wa mji utaanguka chini pale pale. Wanajeshi ni lazime
washambulie, kila mmoja eende mbele moja kwa moja. [6] Ndipo Yoshua mwana wa
Nuni, aliwaita makuhani na kuwaambia, “Lichukueni sanduku la agano, na waacheni
makuhani saba wabebe tarumbeta za pembe za kondoo waume mbele ya sanduku
la Yahweh.” [7] Yoshua aliwaambia watu, “Nendeni na mkatembee kuuzunguka
mji, na watu wa vita wataenda mbele ya sanduku la Yahweh.” [8] Makuhani saba
walibeba tarumbeta saba za pembe za kondoo mbele ya Yahweh kama Yoshua
alivyowaambia watu. Na walivyokuwa akiendelea mbele, walipuliza tarumbeta.
[9] Sanduku la Yahweh liliwafuata kwa nyuma yao. Watu wa vita walitembea mbele
ya makuhani, na walipuliza tarumbeta zao, lakini walinzi wa nyuma walilifuata
sanduku kwa nyuma, na makuhani waliendelea kupuliza tarumbeta zao. [10] Lakini
Yoshua aliwaagiza watu, akisema, “Msipige kelele. Sauti yoyote isitoke vinywani
mwenu mpaka siku nitakayowaambia kupiga kelele. Ndipo hapo mtakapopiga
kelele.” [11] Hivyo, alisababisha sanduku la Yahweh kuuzunguka mji mara moja kwa
siku hiyo. Kisha wakaingia katika kambi yao, wakakaa usiku ule katika kambi.
[12] Basi Yoshua aliamka asubuhi na mapema, na makuhani wakalichukua sanduku la
Yahweh. [13] Makuhani saba waliobeba tarumbeta saba za pembe za kondoo waume
walikuwa mbele ya sanduku la Yahweh, wakitembea kwa ushupavu, huku wakipuliza
tarumbeta. Wanajeshi wenye silaha walikuwa wakitembea mbele yao, lakini walinzi
wa nyuma walitembea nyuma ya sanduku la Yahweh, huku tarumbeta ziliendelea
kupigwa. [14] Walitembea kuuzunguka mji mara moja katika siku ya pili na kisha
wakarudi kambini. Walifanya hivi kwa siku sita. [15] Ilikuwa ni katika siku ya
saba ambayo waliamka mapema katika mapambazuko, na walitembea kuuzunguka
mji kwa namna ile kama ilivyokuwa kawaida yao, katika siku hii walifanya mara
saba. [16] Ilikuwa ni katika siku ya saba ambapo makuhani walipiga tarumbeta, na
ya kwamba Yoshua aliwaagiza watu, “Pigeni kelele! Kwa kuwa Yahweh amewapa
ninyi mji. [17] Mji pamoja na vitu vyote ndani yake vitatengwa kwa Yahweh kwa ajili
ya uharibifu. Ni Rahabu yule kahaba pekee ataishi - yeye pamoja wote waliokuwa
pamoja naye katika nyumba - kwasababu aliwaficha watu tuliowatuma. [18] Lakini
kwenu, iweni waangalifu juu ya kuchukua vitu vilivyotengwa kwa ajili ya uharibifu,
ili baada ya kuvitia alama kwa ajili ya kuharibiwa, msichukue hata kimoja wapo. Na
kama mtafanya hivi, mtaifanya kambi ya Waisraeli iharibiwe na mtaleta matatizo
katika kambi. [19] Fedha zote, dhahabu na vitu vilivyotengenezwa kwa shaba na
chuma vilitengwa kwa ajli ya Yahweh.” [20] Hivyo, watu wakapiga kelele, na wakatoa
sauti kwa kupuliza tarumbeta. Ilikuwa watu waliposikia sauti za tarumbeta, walipiga

kelele kwa sauti kuu, na ukuta ulianguka chini kabisa na kwamba watu waliungia mji,
kila mmoja alisonga mbele moja kwa moja. Na waliuteka mji. [21] Waliteketeza kabisa
kila kitu kilichokuwa katika mji kwa makali ya upanga - wanaume kwa wanawake,
wadogo kwa wakubwa, ng'ombe, kondoo na punda. [22] Kisha Yoshua akawaambia
wale watu wawili walioipeleleza nchi, “Nendeni katika nyumba ya kahaba, mtoeni
mwanamke na wote walio pamoja naye, kama mlivyomwapia.” [23] Basi, vijana wale
walioipeleleza nchi waliingia ndani na kumtoa Rahabu nje. Walimtoa nje baba yake,
mama, kaka, na ndugu wote waliokuwa pamoja naye. waliwaleta katika sehemu
ya nje ya kambi ya Waisraeli. [24] Na ndipo waliuteketeza mji na kila kitu ndani
yake. Isipokuwa fedha, dhahabu na vyombo vya fedha na chuma viliwekwa kwa
hazina ya nyumba ya Yahweh. [25] Bali Yoshua alimruhusu Rahabu kahaba, nyumba
ya baba yake, na wote waliokuwa pamoja naye waishi. Mpaka leo hivi anaishi Israeli
kwasababu aliwaficha watu waliotumwa na Yoshua kuipeleleza Yeriko. [26] Kisha
katika kipindi hicho, Yoshua aliwaamuru kwa kiapo na kusema, “Alaaniwe machoni
pa Yahweh mtu yule anayeujenga mji huu, Yeriko. Ataujenga msingi kwa gharama
ya mzaliwa wake wa kwanza, na kwa gharama ya mzaliwa wake wa pili atapachika
milango yake.” [27] Basi Yahweh alikuwa pamoja na Yoshua, na umaarufu wake ulienea
katika nchi yote.

# 7

[1] Lakini watu wa Israeli hawakutenda katika uaminifu kuhusiana na vitu vilivy-
otengwa kwa ajili ya uharibifu. Akani mwana wa Karmi, mwana wa Zabdi, mwana
wa Zera, kutoka katika kabila la Yuda, alivitwaa baadhi ya vitu hivyo vilivyokuwa
vimetengwa kwa ajili ya uharibifu, na hasira ya Yahweh iliwaka juu yawatu wa
Israeli. [2] Yoshua alituma watu kutoka Yeriko kwenda Ai, mji uliokuwa karibu na
Bethi Aveni, mashariki mwa Betheli. Aliwaambia, “Nendeni na mkaipeleleza nchi.”
Wale watu walikwea na kuipeleleza Ai. [3] Waliporudi kwa Yoshua, walimwambia,
“Usitume watu wote kwenda Ai. Tuma tu watu elfu mbili au elfu tatu waende
kuiteka Ai. Usiwafanye watu wateseke katika vita, kwani ni watu wachache.”
[4] Hivyo ni watu wapatao elfu tatu tu kutoka katika jeshi ndio walioenda, lakini
watu hawa waliwakimbia watu wa Ai. [5] Watu wa Ai waliwaua watu wapatao
thelathini na sita, waliwafuata katika lango la mji hadi katika machimbo ya mawe,
na waliwauwa walipokuwa wakishuka katika kilima. Na mioyo ya watu ilijawa
hofu na ujasiri wao ukawatoka. [6] Basi Yoshua alizirarua nguo zake. Yeye pamoja
na wazewe wa Israeli waliweka mavumbi juu ya vichwa vyao na wakainamisha
vichwa vyao hadi katika nchi mbele ya sanduku la Yahweh, na walibaki pale mpaka
jioni. [7] Kisha Yoshua akasema, “Oo, Yahweh Bwana, kwanini umewavusha watu
hawa ng'ambo ya Yordani? Kutuweka katika mikono ya Waamori ili kutuangamiza?
ikiwa kama tulifanya maamuzi tofauti na tungekaa katika upande mwingine wa
Yordani! [8] Bwana, niseme nini, baada ya Israeli kuwatega migongo maadui zao?
[9] Kwa kuwa Wakaanani na wenyeji wote wa nchi watakaposikia, watatuzunguka na
kuwafanya watu wa nchi kulisahau jina letu. Na utafanya nini kwa ajili ya jina
lako kuu? [10] Yahweh akamwambia Yoshua, “Inuka! kwanini umelala kifudifudi?
[11] Israeli imetenda dhambi. Wamevunja agano langu nililowaagiza. Wameiba baadhi
ya vitu vilivyokuwa vimetengwa. Wameiba na kisha pia wakaficha dhambi yao kwa
kuweka vitu vile walivyochukua miongoni mwa mali zao wenyewe. [12] Na matokeo
yake ni kwamba watu wa Israeli hawataweza kusimama mbele za maadui zao.
Walitega migongo yao kwa maadui zao kwasababu wao wenyewe wametengwa kwa
ajili ya uharibifu. Sitakuwa pamoja nanyi tena mpaka pale mtakapoteketeza vitu
vile vilivyotakiwa kuharibiwa, lakini sasa bado viko miongoni mwenu. [13] Inuka!

Waweke watu wakfu kwangu, na uwaambie, 'Jiwekeeni wakfu ninyi wenyewe
kesho. Kwa kuwa, Yahweh, Mungu wa Israeli asema hivi, "Kuna vitu vilitengwa ili
kuteketezwa ambavyo bado viko miongoni mwenu, Israeli. Hamtaweza kusimama
mbele ya maadui zenu mpaka pale mtakapoviondoa miongoni mwenu vitu vyote
ambavyo vilitengwa kwa ajili ya kuteketezwa." 14 Asubuhi, mtajisogeza wenyewe
kwa makabila. Kabila lile ambalo Yahweh atalichagua litasogea karibu kwa koo
zake. Ukoo ule ambao Yahweh atauchagua lazima usogee karibu kwa nyumba.
Nyumba ambayo Yahweh ataichagua lazima isogee karibu kwa mtu mmoja mmoja.
15 Itakuwa hivi mtu yule atakayechaguliwa na aliye navyo vitu hivyo vilivyotengwa
kwa ajili ya kuharibiwa, atachomwa moto, yeye na kila kitu alichonacho, kwasababu
amelivunja agano la Yahweh na kwasababu amefanya jambo la aibu katika Israeli.'"
16 Basi, Yoshua aliamka asubuhi na mapema na aliwaleta Israeli karibu, kabila kwa
kabila, na kabila la Yuda lilichaguliwa. 17 Yoshua akazisogeza koo za Yuda karibu,
na ukoo wa Zera ulichaguliwa. Akausogeza karibu ukoo wa Zera mtu kwa mtu,
na Zabdi alichaguliwa. 18 Akaisogeza karibu nyumba ya Zabdi mtu kwa mtu, na
Akani mwana wa Karmi, mwana wa Zabdi, mwana wa Zera, kutoka kabila la Yuda,
alichaguliwa. 19 Kisha Yoshua akamwambia Akani, "Mwanangu, niambie ukweli
mbele za Yahweh, Mungu wa Israel, na ufanye ukiri wako kwake. Tafadhali niambie
kile ulichofanya. Usinifiche." 20 Akani akamjibu Yoshua, " Kwa kweli nimetenda
dhambi mbele Yahweh, Mungu wa Israeli. 21 Nilichofanya ni hiki: Nilipoona
miongoni mwa nyara mkoti mzuri kutoka Babeli, shekeli mia mbili za fedha, na
kipande cha dhahabu chenye uzito wa shekeli hamsini, nilivitamani na nikavichukua.
Vimefichwa chini ardhini katikati ya hema langu, na fedha iko chini yake." 22 Yoshua
akatuma wajumbe waliokimbia mpaka kwenye hema mahali palipokuwa na vile
vitu. Walipoangalia, waliviona vimefichwa katika hema lake, na fedha chini yake.
23 Walivichukua vitu hivyo kutoka katikati ya hema na kuvileta kwa Yoshua na watu
wote wa Israeli. Walivimwaga mbele za Yahweh. 24 Kisha Yoshua na Waisraeli wote
pamoja naye, walimchukua Akani mwana wa Zera, na fedha, na koti, na kipande cha
dhahabu, wana na binti zake, ng'ombe zake, punda zake, kondoo zake, hema lake,
na kila kitu alichokuwa nacho, na wakavileta hata bonde la Akori. 25 Kisha Yoshua
akasema, "Kwanini umetusumbua? Leo Yahweh atakutesa na wewe." Waisraeli wote
wakampiga kwa mawe. Na wakawachoma wote kwa moto, na wakawapiga mawe.
26 Kisha wakaweka juu yake kichuguu kikubwa cha mawe ambayo yapo hata leo.
Yahweh akaachilia mbali hasira yake. Hivyo basi, jina la mahali hapo likawa Akori
hata leo.

# 8

1 Yahweh akamwambia Yoshua, "Usiogope; usivunjike moyo. Chukua pamoja
nawe watu wa vita. Pandeni kwenda Ai. Tazama nimemtia mkononi mwako
mfalme wa Ai, watu wake, mji wake na nchi yake. 2 Mtafanya hivyo pia huko
Ai na mfalme wake kama mlivyofanya kwa Yeriko na mfalme wake, isipokuwa
mtachukua nyara na mifugo kwa ajili yenu. Pangeni mashambulizi ya uviziaji
nyuma ya mji." 3 Basi Yoshua aliinuka na akawachukua kwenda Ai watu wote wa
vita. Kisha Yoshua akachagua watu elfu thelathini - wenye nguvu na ujasiri - na
aliwatuma waende wakati wa usiku. 4 Aliwaamuru, "Tazama, mtalala katika hali ya
mashambulizi ya uviziaji dhidi ya mji, kwa nyuma yake. Usiende mbali sana na mji,
lakini ninyi nyote muwe tayari. 5 Mimi pamoja na watu wote walio pamoja nami
tutaukaribia mji. Na wakati watakapokuja kutushambulia sisi, tutawakimbia kama
tulivyofanya hapo mwanzo. 6 Watatoka nje watukimbize mpaka hapo tutakapokuwa
tumewavuta mbali sana na mji, watasema, "Wanatukimbia kama walivyofanya mara
ya mwisho.' Hivyo tutawakimbia na kwenda mbali. 7 Kisha mtapanda kutoka sehemu

mliyojificha, na mtauteka mji. Yahweh Mungu wenu atawapa mkononi mwenu.
[8] Tazama nimewaamuru, mtakapouteka mji, mtauchoma moto. Mtayafanya haya
wakati mtakapotii agizo lililotolewa katika neno la Yahweh." [9] Yoshua akawatuma,
na wakaenda sehemu ya uviziajia, na wakajificha kati ya Betheli na Ai sehemu ya
magharibi ya Ai. Yoshua akalala miongoni mwa watu usiku ule. [10] Yoshua aliamka
asubuhi na mapema na akawaandaa tayari wanajeshi wake, Yoshua na wazee wa
Israeli walishambuliwa watu wa Ai. [11] Watu wote wa vita waliokuwa pamoja naye
walipanda na kuukaribia mji. Walisogea karibu na mji na wakapiga kambi sehemu
ya kasikazini mwa Ai. Kulikuwa na bonde kati yao na Ai. [12] Alichukua watu wapatao
elfu tano hivi na akawaweka katika hali ya kuvizia katika upande wa magharibi
mwa mji kati ya Betheli na Ai. [13] Waliwapanga wanajeshi wote, jeshi kuu katika
upande wa kasikazini mwa mji, na walinzi wa nyuma upande wa magharibi mwa
mji. Yoshua alilala bondeni usiku ule. [14] Na ilikuwa alipoona hilo mfalme wa Ai, yeye
pamoja na jeshi lake, waliamka asubuhi na mapema na walitoka kwa haraka kwenda
kuwashambulia Israeli katika eneo linalokabili bonde la Mto Yordani. Hakujua
kuwa kulikuwa na shambulizi la kuvizia lilikuwa linasubiria kushambulia kutokea
kwa nyuma ya mji. [15] Yoshua na Waisraeli wote walikubali wenyewe kushindwa
mbele yenu, na wakakimbia kuelekea nyikani. [16] Watu wote waliokuwa kwenye
mji waliitwa kwa pamoja waende mbele yao, na walienda mbele ya Yoshua na
kwa jinsi hiyo walivutwa mbali na mji. [17] Hapakuwa na mtu mme aliyesalia Ai
na Betheli ambaye alikuwa hajaenda nje kuwafuatilia waisraeli. Na walipokuwa
wanawafuatilia Waisraeli, Wakatoka na waliuacha mji wazi. [18] Yahweh akamwambia
Yoshua, "Nyosha mkuki huo ulio mkononi mwako kuelekea Ai, kwa kuwa nitaitia Ai
mikononi mwako." Yoshua akaunyosha mkuki uliokuwa mkononi mwake kuuelekea
mji. [19] Wanajeshi waliojificha katika hali ya kuvizia walitoka upesi katika eneo lao
mara tu alipounyosha mkono wake. Walikimbia mbio na kuuingia mji na kuuteka.
Na kwa haraka wakauchoma moto mji. [20] Watu wa Ai waligeuka na kuangalia nyuma.
Waliona moshi kutoka katika mji ukipanda kwenda angani, na hawakuweza kutoroka
kwa njia hii au ile. Kwa kuwa wanajeshi wa Israelei waliokuwa wamekimbia katika
nyika, sasa walirudi kuwakabili wale waliokuwa wanawafuatilia. [21] Na wakati
Yoshua na Israeli wote walipoona kuwa wale watu wa kuvizia wameuteka mji kwa
ule moshi uliokuwa ukipanda, waligeuka nyuma na kuwaua watu wa Ai. [22] Na
wanajeshi wengine wa Israeli, wale waliokuwa wameingia ndani ya mji, walitoka nje
ili kuwashambulia. Hivyo, watu wa Ai walikamatwa katikati ya majeshi ya Israeli,
baadhi katika upande huu na wengine katika upande ule. [23] Lakini walimhifadhi
mfalme wa Ai, ambaye walimteka akiwa hai, na kisha wakamleta kwa Yoshua.
[24] Ilikuwa baada ya Israeli walipokuwa wamemaliza kuuwaua wenyeji wote wa Ai
katika uwanda kariibu na nyika mahali walipowafuata, na baada ya wao wote, hata
yule wa mwisho, walipokuwa wamekwisha kulala kwa ncha ya upanga, Waisraeli
wote walirudi Ai. Waliuteka mji kwa ncha ya upanga. [25] Wale wote walikufa siku hiyo
walikuwa watu elfu kumi na mbili elfu, wanaume na wanawake, wote ni watu wa
Ai. [26] Yoshua hakuukunja mkono wake ambao alikuwa ameunyosha huku akishikilia
mkuki wake, mpaka pale alipowateketeza kabisa watu wote wa Ai. [27] Waisraeli
walichukua tu wanyama na nyara kutoka katika mji kwa ajili yao wenyewe, kama
Yahweh alivyokuwa amemwagiza Yoshua. [28] Yoshua aliichoma Ai na kuigeuza kuwa
kichuguu cha mapango. Ni mahali palipoachwa ukiwa hata leo. [29] Alimtundika
mfalme wa Ai juu ya mti mpaka jioni. Na jua lilipokuwa linaenda kuzama, Yoshua
aliwaagiza na wakautoa mwili wa mfalme wakaushusha chini ya mti na kuutupa
mbele ya malango ya mji. Huko wakaweka kichuguu kikubwa cha mawe juu yake.
Kichuguu hicho kimebaki huko hata leo. [30] Kisha Yoshua akajenga madhabahu kwa

Yahweh, Mungu wa Israeli katika Mlima wa Ebali, 31 kama vile Musa mtumishi wa
Yahweh alivyowaagiza watu wa Israeli, kama ilivyoandikwa katika kitabu cha sheria
ya Musa: "Madhabahu ya mawe yasiyochongwa, ambayo juu yake hakuna mtu
yeyote aliyetumia zana ya chuma." Na allimtolea Yahweh sadaka ya kuteketezwa
juu yake na wakatoa sadaka ya amani. 32 Na huko aliandika juu ya mawe nakala ya
sheria za Musa mbele ya watu wa Israeli. 33 Waisraeli wote, wazee wao, maafisa, na
waamuzi wao walisimama katika sehemu mbili za sanduku mbele ya makuhani na
Walawi ambao hulibeba sanduku la Agano la Yahweh - wageni pamoja na wazalia,
nusu yao walisimama mbele ya Mlima Gerizimu na nusu walisimama mbele ya Mlima
Ebali. Waliwabariki watu wa Israeli kama Musa mtumishi wa Yahweh alivyowaagiza
hapo mwanzo. 34 Baada ya hayo, Yoshua alisoma maneno yote ya sheria, baraka
na laana, kama zilivyoandikwa katika kitabu cha sheria. 35 Halikusalia hata neno
moja katika yote ambayo Musa alimwagiza Yoshua ambalo halikusomwa mbele ya
kusanyiko la Waisraeli lilojumuisha wanawake, watoto wadogo na wageni walioishi
miongoni mwao.

# 9

1 Kisha wafalme wote walioishi ng'ambo ya mto Yordani katika nchi ya milima,
na katika nchi za chini katika pwani za Bahari Kuu mbele ya Lebanoni - Wahiti,
Waamori, Wakanaani, Waperizi, Wahivi na Wayebusi - 2 hawa waliungana pamoja
chini ya amri moja kuinua vita dhidi ya Yoshua na Israeli. 3 Waliposikia wenyeji wa
Gibeoni juu ya mambo aliyoyafanya Yoshua katika Yeriko na Ai, 4 walipanga mpango
wa udanganyifu. Walienda kama wajumbe. Walichukua magunia yaliyochakaa na
kuyaweka juu ya punda. Walichukua pia viriba vilivyochakaa na kuchanika chanika
na vilivyozibwa zibwa. 5 Walivaa miguuni mwao viatu vilivyozeeka na kutoboka
toboka, na walivaa nguo kuukuu, zilichanika chanika. Na mikate yote katika
chombo ilikuwa mikavu na yenye uvundo. 6 Kisha wakamwendea Yoshua katika
kambi huko Giligali na wakamwambia yeye pamoja wa watu wa Israeli wakisema,
" 7 Tumesafiri kutoka nchi ya mbali, basi fanyeni agano nasi." Watu wa Israeli
wakawaamba Wahivi, "Huenda mnaishi karibu nasi. Twawezeje kufanya agano
nanyi?" 8 Wakamwambia Yoshua, "Sisi ni watumishi wako."Yoshua akawauliza,
"Ninyi ni akina nani? Mnatokea wapi? 9 Wakamwambia, "Watumishi wako
wamekuja hapa kutokea nchi ya mbali, kwasababu ya jina la Yahweh Mungu wako.
Tumesikia habari kumhusu na kuhusu kila kitu alichokifanya Misri - 10 na kila
kitu alichokifanya kwa wafalme wawili wa Waamori katika upande mwingine wa
Yordani - kwa mfalme Sihoni wa Heshiboni, na kwa Ogu wa Bashani aliyekuwa
katika Ashitarothi. 11 Wazee wetu na wenyeji wote wa nchi yetu walituambia,"
Chukueni chakula mikononi mwenu kwa ajili ya safari. Nendeni mkakutane nao,
na kisha muwambie, "Sisi ni watumishi wenu. Fanyeni agano pamoja nasi." 12 Huu
ni mkate wetu, ulikuwa wa moto tulipouchukua kutoka katika nyumba zetu katika
siku ile tulipotoka kuja kwenu. Lakini sasa, tazama, imekuwa kavu na yenye
ukungu. 13 Viriba hivi vilikuwa vipya tulipovijaza, na tazama, sasa vinavuja. Nguo
zetu na viatu vyetu vimechakaa na kuwa vikuukuu kwasababu ya safari ndefu."
14 kwahiyo, Waisraeli wakatwaa sehemu ya vyakula vyao, lakini walifanya hivyo
bila ya kumwuliza Yahweh ili awaongoze. 15 Yoshua akafanya amani pamoja nao na
kufanya agano pamoja nao ili waishi. Viongozi wa watu nao pia wakawaapia. 16 Siku
tatu baada ya Waisraeli kufanya agano pamoja nao, waligundua kuwa walikuwa ni
majirani zao na ya kwamba waliishi karibu nao. 17 Kisha watu wa Israeli walisafiri
na kufika katika miji yao katika siku ya tatu. Miji yao ilikuwa Gibeoni, Kefira,
Beerothi, na Kiriathi Yearimu. 18 Watu wa Israeli wahakushambulia kwasababu

viongozi wao walikuwa wamewaapia mbele za Yahweh, Mungu wa Israeli. Waisraeli
wote walikuwa wananung'unika kinyume na viongozi wao. 19 Lakini viongozi wote
waliawaambia watu wote wa Israeli, “Tumeapa kwa Yahweh, Mungu wa Israeli
kwa ajili yao, na sasa hatuwezi kuwadhuru. 20 Hiki ndicho tutakachowafanyia:
Tutawaacha waishi ili tuepuke ghadhabu ambayo yaweza kuja juu yetu kwasababu
ya kiapo tulichowaapia.” 21 Viongozi wakawaambia watu, “Waacheni waishi.”
Hivyo Wagibeoni wakawa wakata kuni na wachota maji wa Waisraeli wote, kama
vile viongozi walivyosema juu yao. 22 Yoshua aliwaita na kuwaambia, “ Kwanini
mlitudanya wakati mliposema, “Tuko mbali sana nanyi' wakati mnaishi hapa hapa
miongoni mwetu? 23 Na kwasababu hii, mmelaaniwa na baadhi yenu mtakuwa
watumwa siku zote, wenye kukata kuni na kuchota maji kwa ajli ya nyumba
ya Mungu wangu.” 24 Walimjibu Yoshua na kusema, “Ni kwasababu watumishi
wako waliambiwa kwamba Yahweh Mungu wenu alimwagiza Musa mtumishi wake
kuwapa ninyi nchi yote, na kuwateteza wenyeji wote wa nchi mbele yenu - hivyo
tuliogopa kwasababu yenu kwa ajili ya maisha yetu. Ndio maana tulifanya jambo
hili. 25 Tazama sasa, mnatumiliki chini ya utawala wenu. Chochote kilichochema
na haki kwenu kutufanyia, fanyeni.” 26 Basi Yoshua aliwafanyia hivi: aliwaondoa
katika mamlaka ya watu wa Israeli, na Waisraeli hawakuwaua. 27 Siku hiyo Yoshua
aliwafanya Wagibeoni kuwa wakata kuni na wachotaji wa maji kwa jamii, na kwa
madhabahu ya Yahweh hadi leo katika sehemu ambayo Yahweh huichagua.

# 10

1 Ikawa Adonizedeki, mfalme wa Yerusalemu, alisikia kuwa Yoshua ameiteka Ai
na ameiteketeza kabisa, kama alivyokwisha kufaya huko Yeriko na mfalme wake.
Na alisikia jinsi ambavyo watu wa Gibeoni walivyofanya amani na watu wa Israeli
na walikuwa wanaishi miongoni mwao. 2 Watu wa Yerusalemu waliogopa sana
kwasababu Gibeoni ulikuwa mji mkubwa, kama mmoja wa miji ya kifalme. Ilikuwa
kubwa kuliko Ai, na watu wake wote walikuwa ni mashujaa wenye nguvu. 3 Hivyo
Adonizedeki, mfalme wa Yerusalemu, alituma ujumbe kwa Hohamu, mfalme wa
Hebroni, na kwa Piramu, mfalme wa Yarimuthi, na kwaYafia, mfalme wa Lakishi,
na kwa Debiri, mfalme wa Eguloni: 4 “Njooni kwangu na mnisaidie. Tuishambulie
Gibeoni kwasababu wamefanya amani na Yoshua pamoja na watu wa Israeli.
5 Wafalme watano wa Waamori; mfalme wa Yerusalemu, mfalme wa Hebroni,
mfalme wa Yarimuthi, mfalme wa Lakishi, na mfalme wa Eguloni walikwea, wao
pamoja na majeshi yao yote. Walipanga sehemu yao kinyume na Wagibeoni na
waliwashambulia. 6 Watu wa Gibeoni walituma ujumbe kwa Yoshua na kwa jeshi
huko Giligali. Walisema, “ Upesi! Msiuondoa mkono wenu kutoka kwa watumishi
wenu. Kwaeni mje haraka na mtuokoe. Mtusaide, maana wafalme wote wa Waamori
wanaoishi katika nchi ya milima wamekusanyika kwa pamoja ili watushambulie.
7 “Yoshua alipanda kutoka Giligali, yeye na watu wote wa vita pamoja naye, na watu
wote wapiganaji. 8 Yahweh akamwambia Yoshua, “Usiwaogope. Nimewatiwa wote
katika mkono wako. Hakuna hata mmoja wao atakayeweza kuzuia mashambulizi
yako.” 9 Baada ya kutembea usiku kucha kutoka Giligali, ghafla Yoshua aliwafikilia.
10 Na Yahweh alichanganya maadui mbele za Israeli - ambao waliwaua mauaji
makubwa mno huko Gibeoni, na wale waliowafuata njiani iendayo Bethi Horoni,
nao waliuwaua katika njia iendayo Azeka na Makeda. 11 Na walipokuwa wakikimbia
mbio kutoka kwa Waisraeli, chini ya mlima kutoka Bethi Horoni, Yahweh alitupa
mawe makubwa kutoka mbinguni juu yao wote katika njia iendayo Azeka, nao
wakafa. Watu waliouawa kwa mawe walikuwa ni wengi zaidi kuliko wale waliouawa
kwa upanga wa watu wa Israeli. 12 Kisha Yoshua akamwambia Yahweh katika siku

ambayo Yahweh aliwapa watu wa Israeli ushindi dhidi ya Waamori. Hiki ndicho
Yoshua alichosema kwa Yahweh mbele ya Israeli. " Jua lisimame katika Gibeoni,
na mwezi, usimame katika bonde la Aijaloni." 13 Jua lilisimama, na mwezi ukaacha
kwenda mpaka taifa lilipolipiza kisasi dhidi ya maadui zao. Je hili halikuandikwa
katika Kitabu cha Yashari? Jua lilikaa katikati ya anga; halilkuzama kwa siku
nzima hivi. 14 Haijawahi kutokea siku nyingine kama hiyo kabla au baada yake,
wakati Yahweh alipotii sauti ya mtu. Kwa kuwa Yahweh alikuwa akifanya vita
badala ya Israeli. 15 Yoshua na Israeli yote pamoja naye walirudi kambini huko
Giligali. 16 Basi wale wafalme watano walikuwa wametoroka na kujificha wao
wenyewe katika pango huko Makeda. 17 Taarifa zilimfikia Yoshua kusema, "Wafalme
watano wamepatikana wamejificha katika pango huko Makeda!" 18 Yoshua akasema,
"Viringisheni mawe makubwa katika mlango wa pango na muweke wanajeshi hapo
ili kuwalinda. 19 Msibaki na kukaa nyie wenyewe. Bali wafuatilieni maadui zenu
na kuwashumbulia kutokea kwa nyuma. Msiwaruhusu kuingia katika miji yao,
kwa kuwa Yahweh Mungu wenu amewatia katika mkono wenu." 20 Yoshua na
wana Waisraeli walikuwa wamemaliza kuwaua kwa mauaji makubwa sana, mpaka
pale walipokuwa wameteketezwa kabisa; watu wachache tu walipona waliotoroka
walifika miji ya ngome. 21 Kisha jeshi lote lilirudi kwa Yoshua likiwa na amani
katika kambi huko Makeda. Na hakuna hata mmoja aliyethubutu kusema hata neno
moja kinyume na watu wa Israeli. 22 Kisha Yoshua akasema, "Fungueni mlango
wa pango, watoeni nje na waleteni kwangu hawa wafalme watano." 23 Walifanya
kama Yoshua alivyosema. Waliwaleta wafalme watano kutoka katika pango - mfalme
wa Yerusalemu, mfalme wa Hebroni, mfalme wa Yarmuthi, mfalme wa Lakishi na
mfalme wa Egloni. 24 Na walipowaleta wafalme kwa Yoshua, alimwita kila mtu wa
Israeli, na aliwaambia maakida wa wanajeshi waliokuwa wameenda vitani pamoja
naye " Kanyageni miguu yenu juu ya shingo zao." Basi walikuja na kukanyaga
miguu yao juu ya shingo zao. 25 Kisha akawaambia, 'Msiogope wala kufadhaika.
uwe na moyo mkuu na jasiri. Na hiki ndicho Mungu atakachokifanya kwa maadui
wenu wote ambao mtapigana nao'. 26 Kisha Yoshua akawashambulia na kuwaua
wafalme. Aliwatundika wote watano juu ya miti. Waliwatundika juu ya miti hata
jioni. 27 Ilipokuwa jioni, Yoshua alitoa maagizo, nao waliwashusha chini ya miti
na kisha wakawatupa katika pango ambalo walikuwa wamejificha wao wenyewe.
Waliweka mawe makubwa juu ya mlango wa pango. Mawe hayo yapo pale hadi
leo hii. 28 Na kwa namna hii, katika siku hiyo Yoshua aliuteka mji wa Makeda
na aliwaua watu wote huko kwa upanga, pamoja na mfalme wake. Aliwateketeza
wote kabisa pamoja na kila kiumbe hai kilichokuwa huko. Hakuna hata mmoja
aliyesalia. Alichomfanyia mfalme wa Makeda ni sawa sawa na kile alichokuwa
amemfanyia mfalme wa Yeriko. 29 Yoshua na Israeli wote waliipita Makeda na kufika
Libna. Na huko waliingia katika vita dhidi ya Libna. 30 Yahweh pia aliitia katika
mkono wa Israeli pamoja na mfalme wake. Yoshua alishambulia kila kiumbe hai
ndani yake kwa upanga. Hakuacha hai hata mtu mmoja. Alichomfanyia mfalme ni
sawa sawa na kile alichokuwa amemfanyia mfalme wa Yeriko. 31 Baadaye Yoshua
na Israeli wote pamoja naye walipanda kutoka Libna na kwenda Lakishi. Alipiga
kambi karibu yake na wakafanya vita dhidi yake. 32 Yahweh aliitia Lakishi katika
mkono wa Israeli. Yoshua aliiteka katika siku ya pili. Alishambulia kwa upanga
kilia kiumbe hai kilichokuwa ndani yake, kama vile aliyokuwa amefanya huko
Libna. 33 Kisha Horamu, mfalme wa Gezeri alikwea ili kuisaida Lakishi. Yoshua
alimshambulia yeye na jeshi lake mpaka pale ambapo hapakuwa na mtu hata mmoja
aliyesalia. 34 Baada ya hapo, Yoshua na Israeli wote walitoka Lakishi na kwenda
Egloni. Walipiga kambi karibu yake na kisha wakafanya vita dhidi yake, 35 na

siku hiyo hiyo wakaiteka. Waliupiga kwa upanga na waliteketeza kila mtu ndani
yake kama vile Yoshua alivyofanya huko Lakishi. 36 Kisha Joshua na Israeli wote
wakatoka Egloni na kwenda Hebroni. Wakainua vita dhidi yake. 37 Waliuteka mji na
kuwaua kwa upanga watu wote ndani yake pamoja na mfalme wake, kujumuisha
na vijiji vyote vilivyoizunguka. Waliteketeza kabisa kila kiumbe hai ndani yake,
hawakuacha hata mtu mmoja aliyesalia, ni sawa sawa na vile Yoshua alivyoitenda
Egloni. Aliiteketeza kabisa, na kila kiumbe hai ndani yake. 38 Baada ya hapo, Yoshua
alirudi pamoja na jeshi lote la Israeli pamoja naye, wakasafiri kwenda Debiri na
kufanya vita dhidi yake. 39 Aliuteka mji na mfalme wake, pamoja na vijiji vyake
vya jirani. Waliwaua wote kwa upanga na waliteketeza kila kiumbe hai ndani
yake. Joshua hakuacha hata mmoja hai, kama alivyokuwa amefanya kwa Hebroni na
mfalme wake, na kama alivyokuwa amefanya kwa Libna na mfalme wake. 40 Yoshua
aliishinda nchi yote, nchi ya milima, Negevu, nchi, nchi ya tambarare na nchi ya
miteremko. Hakuna hata mfalme moja aliyebaki hai kati ya wafalme wake wote.
Kwa kweli aliteketeza kila kiumbe hai, kama ambavyo Yahweh, Mungu wa Israeli
alivyomwaagiza. 41 Yoshua aliwaua kwa upanga kutoka Kadeshi Barnea hadi Gaza,
na nchi yote ya Gosheni hata Gibeoni. 42 Yoshua aliwateka wafalme wote hawa na
nchi zao kwa wakati mmoja, kwasababu Yahweh, Mungu wa Israeli, alipigana kwa
ajili ya Israeli. 43 Baada ya hayo Yoshua na Waisraeli wote pamoja naye, walirudi
katika kambi huko Gilgali.

# 11

1 Basi ikawa aliposikia haya, Yabini, mfalme wa Hazori, alituma ujumbe kwa
Yobabu, mfalme wa Madoni, na kwa mfalme Shimroni, na kwa mfalme wa Akshafu.
2 Alituma pia ujumbe kwa wafalme walikuwa katika mlima wa kaskazini mwa nchi,
katika bonde la Mto Yordani kusini mwa Kinerethi, katika nchi za tambarare, na
katika nchi za milima ya Dori kuelekea magharibi. 3 Pia, alituma ujumbe kwa
Wakanaani walioko mashariki na magharibi, Waamori, Wahiti, Waperizi, Wayebusi
katika nchi za milima, na Wahivi karibu na Mlima Hermoni katika nchi ya Mizipa.
4 Maadui zao wote walitoka pamoja nao, wanajeshi wengi sana, hesabu yao ilikuwa
kama mchanga wa pwani. Walikuwa na farasi wengi sana na magari. 5 Wafalme
wote hawa walikutana katika muda waliokuwa wameupanga, na walipiga kambi
katika maji ya Meromu ili kupigana vita na Israeli. 6 Yahweh akamwambia Yoshua,
“Usiogope mbele zao, kwa kuwa muda kama huu kesho ninawatia hao kwa Waisraeli
wakiwa wafu. Utaivunja vunja miguu ya farasi zao, na utayachoma moto magari
yao.” 7 Yoshua na watu wote wa vita walitoka na mara wakafika katika maji
ya Meromu, na wakawashambulia maadui. 8 Yahweh akawatia maadui katika
mkono wa Israeli, na waliwapiga kwa upanga na wakawafuata mpaka Sidoni,
Misrefothi - Maimu, na katika bonde la Mizipa upande wa mashariki. Waliwaua
wote hakuna hata mmoja aliyeachwa hai. 9 Yoshua aliwatendea kama vile Yahweh
alivyomwambia. Alivunja miguu ya farasi na magari aliyachoma moto. 10 Kwa
wakati huo, Yoshua alirudi na akauteka mji wa Hazori. Alimwua mfalme wake
kwa upanga (Hazori ulikuwa ni kichwa cha falme hizi zote). 11 Waliwapiga kwa
upanga kila kiumbe chenye uhai kilichokuwa huko, na alivitenga ili viteketezwe,
hivyo hapakuwa na kiumbe hai kilichoachwa hai. Na kisha aliuchoma moto Hazori.
12 Yoshua aliiteka miji yote ya wafalme hawa. Aliwateka pia wafalme wake wote
na akawapiga wote kwa upanga. Aliwateketeza kabisa kwa upanga, kama Musa
mtumishi wa Yahweh alivyoagiza. 13 Waisraeli hawakuchoma moto mji wowote
miongoni mwa miji iliyojengwa juu ya vilima vya vifuasi vya udongo, isipokuwa
Hazori, ndio mji pekee ambao Yoshua aliuchoma kwa moto. 14 Jeshi la Israeli

lilichukua nyara kutoka katika miji pamoja na mifugo kwa ajili yao wenyewe. Waliua
kila mtu kwa upanga hadi pale walipokufa wote. Hakuna kiumbe hai kilichoachwa
hai. [15] Kama vile Yahweh alivyomwagiza mtumishi wake Musa, na kwa namna
hiyo hiyo, Musa alivyomwagiza Yoshua. Na katika mambo yote ambayo Yahweh
alimwamuru Musa kuyafanya, Yoshua hakuacha kufanya hata jambo moja. [16] Yoshua
alitwaa nchi hiyo yote, nchi ya milima, Negevu yote, nchi yote ya Gosheni, nchi ya
vilima vidogo, bonde la Mto Yordani, nchi ya milima ya Israeli, na nchi tambarare.
[17] Kutoka Mlima Halaki karibu na Edomu, kuelekea kasikazini hadi Baali Gadi katika
bonde karibu na Lebanoni chini ya Mlima Hermoni, aliwateka wafalme wake wote na
kuwaua. [18] Yoshua alipigana vita na wafalme wote kwa muda mrefu. [19] Hakuna hata
mji mmoja uliofanya amani na jeshi la Israeli isipokuwa Wahivi walioishi Gibeoni.
Israeli ilitwaa miji yote iliyosalia katika vita. [20] Kwa kuwa alikuwa ni Yahweh
ambaye alikuwa ameifanya kuwa migumu mioyo yao ili wapande na kufanya vita
dhidi ya Israeli, ili kwamba aweze kuwaangamiza kabisa, na kutowaonesha huruma,
kama alivyomwaagiza Musa. [21] Kisha Yoshua akaja kwa wakati ule na aliiangamiza
Anakimu. Aliyafanya haya katika nchi ya milima, huko Hebroni, Debiri, Anabu,
na katika nchi yote ya Yuda, na katika nchi yote ya milima ya Israeli. Yoshua
aliwaangamiza kabisa pamoja na miji yao. [22] Hakuna hata mmoja wa watu wa
Anakimu aliyeachwa katika nchi ya Israeli, isipokuwa huko Gaza, Gathi na Ashidodi.
[23] Hivyo Yoshua aliiteka nchi yote, kama vile Yahweh alivyomwambia Musa. Yoshua
aliwapa Israeli kama urithi, kila kabila lilipewa sehemu yake. Kisha nchi ikapumzika
bila vita.

# 12

[1] Basi hawa ndio wafalme wa nchi, ambao watu wa Israeli walishindwa. Waisraeli
walichukua miliki ya nchi katika upande wa mashariki mwa Yordani sehemu ambako
jua huchomoza, kutoka bonde la Mto Arnoni hadi Mlima Hermoni, na nchi yote
ya Araba kuelekea kusini. [2] Sihoni, mfalme wa Waamori, aliishi katika Heshiboni.
Alitawala kutoka Aroeri, ambayo iko juu ya bonde la Arnoni kutoka katikati ya
bonde, na nusu ya Geleadi kushuka mpaka Mto Yaboki katika mpaka wa Waamori.
[3] Sihoni pia alitawala juu ya Araba mpaka Bahari ya Kinerethi, kwenda mashariki,
kuelekea Bahari ya Araba (Bahari ya Chumvi) upande wa mashariki, hadi huko Bethi
Yeshimothi na upande wa kusini, kuelekea chini ya miteremko wa Mlima Pisiga.
[4] Ogu, mfalme wa Bashani, mmoja kati ya mabaki ya Rephaimu, aliyeishi huko
Shatarothi na Edrei. [5] Alitawala juu ya Mlima Hermoni, Saleka, na Bahani yote, hadi
mpaka wa watu wa Geshuri na Wamakathi, na nusu ya Gleadi, hadi kufika mpaka
wa Sihohi, mfalme wa Heshboni. [6] Musa mtumishi wa Yahweh, na watu wa Israeli
walikuwa wamewashinda, na Musa mtumishi wa Yahweh aliwapa nchi kama mali
ya Wareubeni, Wagadi na nusu ya kabila la Manase. [7] Hawa ndio wafalme wa nchi
ambayo Yoshua na watu wa Israeli waliwashinda katika upande wa magharibi mwa
mto Yordani, kutoka Baali Gadi katika bonde karibu na Lebanoni hadi Mlima Halaki
karibu na Edom. Yoshua aliyapa nchi makabila ya Israeli ili yaimiliki. [8] Aliwapa nchi
ya milima, tambarare, Araba, sehemu za milima, nyika na Negevu, nchi ya Wahiti,
Waamori, Wakanaani, Waperizi, Wahivi, na Wayebusi. [9] Wafalme hawa walikuwa ni
mfalme wa Yeriko, mfalme wa Ai iliyo karibu na Betheli, [10] mfalme wa Yerusalemu,
mfalme wa Enaimu, [11] mfalme wa Yarmuthi, mfalme wa Lakishi, [12] mfalme wa
Egloni, mfalme wa Gezeri, [13] mfalme wa Debiri, mfalme wa Gederi, [14] mfalme wa
Horima, mfalme wa Aradi, [15] mfalme wa Libna, mfalme wa Adula, [16] mfalme wa
Makeda, mfalme wa Betheli, [17] mfalme wa Tapua, mfalme wa Heferi, [18] mfalme wa
Afeki, mfalme wa Lasharoni, [19] mfalme wa Madoni, mfalme wa Hazori, [20] mfalme wa
Shimroni - Meroni, mfalme wa Akshafu. [21] mfalme wa Taanaki, mfalme wa Megido,

22 mfalme wa Kedeshi, mfalme wa Jokineamu katika Karmeli, 23 mfalme wa Dori
katika Nafutali Dori, mfalme Goyimu katika Giligali, na 24 mfalme Tiriza. Hesabu ya
wafalme ilikuwa ni thelathini na moja kwa ujumla wake.

# 13

1 Sasa Yoshua alikuwa mzee wakati Yahweh alipomwambia, "Umekuwa mzee,
lakini bado kuna nchi kubwa ya kuteka. 2 Nchi iliyosalia ndio hii: mikoa yote
ya Wafilisti, na mikoa ile ya Wageshuri, 3 (tangu Shihori, iliyoko mashariki mwa
Misri, na upande wa kaskazini kuelekea mpaka wa Ekroni, inayofikiriwa kuwa
ni mali ya Wakanaani; wafalme watano wa Wafilisti, wale wafalme wa Gaza,
Ashidodi, Ashikeloni, Gathi na Ekroni - miliki ya Waavi. 4 Katika upande wa kusini,
kulisalia nchi yote ya Wakanaani, na Meara ambayo ni miliki ya Wasidoni, hadi
Afeki, hata mpaka wa Waamori; 5 nchi ya Wagebali, Lebanoni kuelekea upande
wa mapambazuko ya jua, kutoka Baali- Gadi chini ya Mlima Hermoni mpaka Lebo
Hamathi. 6 Pia, wenyeji wote wa nchi ya milima kutoka Lebanoni hadi Misrefothi -
Maimu, pamoja na watu wa Sidoni. Nitawafukuza mbele ya jeshi la Israeli. Uwe na
uhakika wa kuwapa Waisraeli nchi kama urithi, kama nilivyokuagiza. 7 Igawanye
nchi hii kama urithi kwa makabila tisa na kwa nusu ya kabila la Manase. 8 Pamoja
na nusu nyingine ya kabila la Manase, Wareubeni na Wagadi wamekwisha kupokea
urithi wao ambao Musa aliwapa katika upande wa mashariki wa Yordani, 9 kutoka
Aroeri, iliyo katika ukingo wa bonde la mto Arnoni (kujumuisha na mji ambao
uko katikati ya bonde), kwa nyanda zote za Medeba hadi Diboni; 10 miji yote ya
Sihoni, mfalme wa Waamori, ambaye alitawala katika Heshiboni, hata mpaka wa
Waamori, 11 Gileadi na mkoa wa Wageshuri na Maakathi, mlima wote wa Hermoni,
Bashani yote mpaka Saleka; 12 ufalme wote wa Ogu katika Bashani, aliyetawala
katika Ashitarothi na Edrei - hawa ni wale waliosalia katika Refaimu - ambao
Musa aliwapiga na kuwafukuzia mbali. 13 Lakini watu wa Israeli hawakuwafukuza
Wageshuri wala Wamakathi. Badala yake, Wageshuri na Wamakathi wanaishi
miongoni mwa Waisraeli hadi leo. 14 Kabila la Lawi pekee halikupewa urithi na
Musa. Urithi wao ni sadaka za Yahweh, Mungu wa Israeli, zilizotolewa kwa moto,
kama Mungu alivyomwagiza Musa. 15 Musa aliwapa urithi kabila la Rubeni, ukoo kwa
ukoo. 16 Miliki yao ilikuwa kutoka Aroeri, juu ya ukingo wa bonde la Mto Arnoni,
na mji ulio katikati ya bonde, na nyanda zote za Medeba. 17 Wareubeni walipata pia
Heshiboni, na miji yake yote zilizo katika uwanda, Diboni, na Bamathi Baali, na Bethi
Baalimeoni, 18 na Yahazi, na Kedemothi, na Mefaathi, 19 na Kiriathaimu, na Sibuma,
na Zerethishahari juu ya kilima cha bonde. 20 Wareubeni walipata pia Bethi Peori,
miteremko ya Pisiga, Bethi Yeshimothi, 21 miji yote ya uwanda, na ufalme wote wa
Sihoni, mfalme wa Waamori, ambaye alikuwa ametawala katika Heshiboni, ambaye
Musa alikuwa amemshinda pamoja na viongozi wa Midiani, Evi, Rekemu, Zuri, Huri
na Reba, wana wa mfalme wa Sihoni, ambao walikuwa wameishi katika nchi. 22 Pia,
watu wa Israeli walimwua kwa upanga Baalam mwana wa Beori, ambaye alifanya
mambo ya uaguzi, miongoni mwa wale waliowaua. 23 Mpaka wa kabila la Rubeni
ni Mto Yordani; huu ndio mpaka wao. Huu ulikuwa ni urithi wa kabila la Rubeni,
uliotolewa kwa kila ukoo, pamoja na miji na vijiji vyao. 24 Hiki ndicho Musa alilipa
kabila la Gadi, ukoo kwa ukoo: 25 Himaya yao ilikuwa Yazeri, miji yote ya Gileadi
na nusu ya nchi ya Waamoni, hadi Aroeri, iliyo mashariki mwa Raba, 26 kutoka
Heshiboni hadi Ramathi - Mizipe na Betonimu, kutoka Mahanaimu mpaka himaya
ya Debiri. 27 Katika bonde, Musa aliwapa Bethi -Haramu, Bethi - Nimra, Sukothi,
na Zafoni, ufalme uliobakia wa Sihoni mfalme wa Heshiboni, pamoja na Yordani
kama mpaka, katika sehemu za chini za mwisho wa Bahari ya Kinerethi, upande

wa mashariki ng'ambo ya Yordani. 28 Huu ni urithi wa kabila la Gadi, ukoo kwa
ukoo, pamoja na miji na vijiji vyao. 29 Musa aliwapa urithi nusu ya kabila la Manase.
Urithi uligawiwa kwa nusu ya kabila la watu wa Manase kutokana na kabila zao.
30 Miliki yao ilikuwa kutoka Mahanaimu, Bashani yote, ufalme wote wa mfalme Ogu
wa Bashani, na miji yote ya Yairi, iliyo katika Bashani, miji sitini; 31 nusu ya Gileadi,
na Ashitarothi na Edrei (miji ya kifalme ya Ogu katika Bashani). Miji hii iligawanywa
kwa ukoo wa Makiri mwana wa Manase -nusu ya watu wa Makiri, walipewa kwa kila
familia zao. 32 Huu ndio urithi ambao Musa aliowagawia katika nyanda za Moabu,
ng'ambo ya Yordani mashariki mwa Yeriko. 33 Musa hakulipa urithi kabila la Lawi.
kwa kuwa Yahweh, Mungu wa israeli, ni urithi wao, kama vile alivyowaambia.

# 14

1 Maeneo haya ya nchi ambayo watu wa Israeli waliyapokea kama urithi wao katika
nchi ya Kanaani. Urith huu uligawanywa kwao na Eliazeri kuhani, na Yoshua mwana
wa Nuni, na viongozi wa makabila ya mababu wa familia zao kati ya watu wa Israeli.
2 Urithi wao ulichaguliwa kwa kupiga kura kwa makabila tisa na nusu, kama vile
Yahweh alivyoagiza kwa mkono wa Musa. 3 Kwa kuwa Musa alikuwa amewapa
urithi makabila mawili na nusu ng'ambo ya Yordani, lakini Walawi hawakupewa
urithi wowote. 4 Kabila la Yusufu kwa uhalisia yalikuwa makabila mawili, Manase
na Efraimu. Na hakuna sehemu yoyote ya urithi waliyopewa Walawi katika nchi,
lakini walipewa miji ya kuishi ndani yake pamoja na sehemu ya malisho ya mifugo
yao na kwa ajili ya riziki zao. 5 Watu wa Israeli walifanya hivyo kama vile Yahweh
alivyomwagiza Musa, basi waliiganywa nchi. 6 Kisha kabila la Yuda lilikuja kwa
Yoshua huko Giligali. Kalebu mwana wa Yefune Mkenizi, akamwambia,"Unajua
kile Yahweh alichomwambia Musa mtu wa Mungu juu yako na mimi huko Barnea.
7 Nilikuwa na umri wa miaka arobani wakati Musa mtumishi wa Yahweh aliponituma
kutoka Kadeshi Barnea kuipeleleza nchi. Nilimletea taarifa tena kama nilivyotakiwa
kufanya katika moyo wangu. 8 Lakini ndugu zangu walioenda pamoja nami
waliifanya mioyo ya watu iyeyuke kwa woga. Lakini mimi nilimfuata Yahweh kabisa.
9 Musa aliapa katika siku hiyo akisema, "Hakika nchi ambayo miguu yako imetembea
juu yake itakuwa urithi wako na kwa watoto wako milele, kwasababu umemfuata
kabisa Yahweh Mungu wangu. 10 Tazama! sasa, Yahweh amenihifadhi hai kwa miaka
hii arobaini na tano, kama alivyosema - tangu kipindi kile Yahweh alivyomwambia
Musa neno hili, wakati huo Waisraeli walikuwa wakitembea jangwani. Tazama! sasa
katika siku hii ya leo nina miaka themanini na mitano. 11 Bado hata siku hii ya leo
nina nguvu kama nilivyokuwa katika siku ile ambayo Musa alinituma. Nguvu zangu
za sasa ni sawa na nguvu zangu za kipindi kile, kwa ajili ya vita na kwa kwenda
na kwa kuja. 12 Sasa basi, nipe nchi hii ya milima, ambayo Yahweh aliniahidi katika
siku hiyo. Kwa kuwa ulisikia katika siku hiyo kuwa Wanakimu walikuwa huko katika
miji yenye ngome. Itakuwa kwamba Yahweh atakuwa pamoja nami na ya kwamba
nitawafukuzia mbali, kama vile Yahweh alivyosema." 13 Kisha Yoshua alimbariki
Kalebu mwana wa Yefune na alimpa Hebroni kama urithi wake. 14 Hivyo Hebroni
ikawa urithi wa Kalebu mwana wa Yefune Mkenizi hata leo, kwasababu alimfuata
kabisa Yahweh, Mungu wa Israeli. 15 Basi, jina la Hebroni hapo mwanzo lilikuwa ni
Kiriathi Arba ( Arba ambaye alikuwa ni mtu mkuu miongoni mwa Wanakim). Kisha
nchi ikawa na raha bila vita.

# 15

1 Ugawanaji wa nchi kwa kabila la watu wa Yuda, walipewa kwa kufuatana na
koo zao, kutoka upande wa kusini hadi mpaka wa Edomu, pamoja na nyika ya

Sini iliyokuwa mbali sana kuelekea kusini. 2 Mpaka wao wa upande wa kusini
ulianzia mwisho wa Bahari ya Chumvi, kutoka ghuba iliyokabili upande wa kusini.
3 Mpaka wao mwingine ulielekea upande wa kusini wa mlima wa Akrabimu na
kupita kuelekea Sini, na kupanda upande wa Kadeshi Barnea, karibu na Hezroni,
hadi Addari mahali ambapo ulipinda kuelekea Karika. 4 Ulipita katika Azimoni,
kuelekea kijito cha Misri, na mwisho ulikuwa katika bahari. Huu ulikuwa ni mpaka
wa kusini. 5 Mpaka wa mashariki ulikuwa ni Bahari ya Chumvi, katika mdomo wa
Yordani. Mpaka wa upande wa kasikazini ulianzia katika ghuba ya bahari katika
mdomo wa Yordani. 6 Ulielekea mpaka Bethi Hogla na ulipita kaskazini mwa Bethi
Araba. Kisha ulipanda hata JIwe la Bohani mwana wa Rubeni. 7 Basi mpaka ule
ulienda hadi Debiri kutoka katika bonde la Akori, kuelekea upande wa kasikazini,
kuendelea hadi Giligali, ambayo iko mkabala na mlima Adumimu, iliyo upande wa
kusini wa bonde. Kisha mpaka uliendelea hata katika chemichemi za Eni Shemeshi
na kufika Eni Rogeli. 8 kisha mpaka ulishuka hadi bonde la Beni Hinomu kuelekea
upande wa kusini wa mji wa Wayebusi ( ambao ni Yerusalemu). Kisha ulipanda
hata katika mlima ulio juu ya bonde la Hinomu, katika upande wa magharibi, ulio
mwishoni mwa bonde la Refaimu katika upande wa kasikazini. 9 Kisha mpaka
ulitanuka kutoka katika kilele cha milima hata chemichemi ya Nefutoa, na ulipanda
kutoka hapo kuelekea miji ya Mlima Efroni. Kisha mpaka ulipiga kona kuelekea
Baala ( ambao ndio Kiriathi Yearimu). 10 Baadaye mpaka ulizunguka kuelekea
magharibi mwa Baala kukabili Mlima Seiri, na kupita kufuata upande wa Mlima wa
Yearimu katika upande wa kasikazini (ambao ndio Kesaloni), ulienda chini hadi Bethi
Shemeshi na kuvuka hata ng'ambo ya Timna. 11 Mpaka uliendelea karibu na mlima
wa kasikazini mwa mlima wa Ekroni, na kisha ukakata kona kuzunguka Shikeroni na
kupita kuelekea sambasamba na Mlima Baala, kutoka hapo uliendelea hadi Yabneeli.
Mpaka ule ulikomea katika bahari. 12 Mpaka wa magharibi ulikuwa Bahari Kuu na
katika ukanda wa pwani yake. Huu ndio mpaka uliozunguka kabila la Yuda, ukoo
kwa ukoo. 13 Katika kulitunza agizo la Yahweh kwa Yoshua, Yoshua alimpa Kalebu
mwana wa Yefune mgao wa nchi ya. miongoni mwa kabila la Yuda, alimgawia nchi
Kiriathi Arba, ambayo ndio Hebroni (Arba alikuwa ni baba wa Anaki). 14 Kalebu
aliwafukuzia mbali wana watatu wa Anaki: Sheshai, Ahimani na Talmai, wazawa wa
Anaki. 15 Alipanda kutoka pale kinyume cha wenyeji wa Debiri (Debiri hapo mwanzo
iliitwa Kiriathi Seferi). 16 Kalebu akasema, “Mtu atakayeishambulia Kiriathi Seferi
na kuiteka, nitampa binti yangau, Akisa, awe mke wake. 17 Wakati huo Othinieli
mwana wa Kenazi, kaka yake na Kalebu, aliuteka mji, na Kalebu alimpatia Akisa,
binti yake awe mke wake. 18 Mara baada ya hayo, Akisa aliend kwa Othinieli na
alimsihi amwombe baba yake shamba. Na mara aliposhuka kutoka katika punda
wake, Kalebu alimwambia Akisa, “Unataka nini?” 19 Akisa akamjibu, “Nifanyie
neema. Kwa kuwa umeshanipa nchi ya Negevu, nipe pia baadhi ya chemichemi
za maji.” Na Kalebu alimpa chemichemi ya juu na chemichemi ya chini. 20 Huu
ulikuwa ndio urithi wa kabila la Yuda, waliopewa kufuatana na koo zao. 21 Miji
iliyo mali ya kabila la Yuda katika upande wa kusini, kuelekea mpaka wa Edomu,
ilikuwa ni Kabzeeli, Eda, Yaguri, 22 Kina, Dimona, Adada, 23 Kadeshi, Hazor, Ithinani,
24 Zifu, Telemu, Bealothi. 25 Hazori Hadata, Keriothi Hezroni (mji huu ulijulikana
kama Hazori), 26 Amamu, shema, Molada, 27 Hazari Gada, Heshimoni, Bethi Peleti,
28 Hazari Shuali, Beerisheba, Biziothia. 29 Baala, Limu, Ezemu, 30 Eltoladi, Kesili,
Horma, 31 Ziklagi, Madimana, Sansana, 32 Lebaothi, Shilihimu, Aini, na Rimoni. Miji
hii ilikuwa ishirini na tisa kwa ujumla, kujumlisha na vijiji vyake. 33 Katika nchi
iliyo chini ya mlima upande wa magharibi, kulikuwa na miji ya Eshtaoli, Zora,
Ashina, 34 Zanaoa, Eni Ganimu, Tapua, Enamu, 35 Yarmuthi, Adulamu, Soko, Azeka,

36 Shaaraimu, Adithaimu, na Gedera ( ambayo ndio Gederothaimu). Hesabu ya miji
hii ilikuwa ni kumi na nne, pamoja na vijiji vyao. 37 Zena, Hadasha, Migidagadi,
38 Dileani, Mizipa, Yokitheeli, 39 Lakishi, Bozikathi, Egloni. 40 Kaboni, Lahmamu,
Kitilishi, 41 Gederothi, Bethi Dagoni, Naama, Makeda. Hesabu ya miji hii ilikuwa
kumi na sita, kujumlisha na vijiji vyao. 42 Libna, Etheri, Ashani, 43 Ifuta, Ashina,
Nezibu, 44 Keila, Akizibu, na Maresha. Hii ilikuwa ni miji tisa, kujumlisha na vijiji
vyao. 45 Ekroni, pamoja na miji na vijiji vyake vinavyoizunguka; 46 kutoka Ekroni
kuelekea Bahari Kuu, makazi yote ambayo yalikuwa karibu na Ashidodi, pamoja na
vijiji vyake. 47 Ashidodi, na miji na vijiji vyake vinavyoizunguka; Gaza na miji na
vijiji vyake vinavyoizunguka; hata kufika kijito cha Misri, na kuelekea Bahari Kuu
pamoja na ukanda wake wa pwani. 48 Katika nchi ya milima, kuna miji ya Shamiri,
Yatiri, Soko, 49 Dana, Kiriathi Sana (ambayo ndio Debiri), 50 Anabu, Eshitemo, Animu,
51 Gosheni, Holoni, na Gilo. Hii ilikuwa ni miji kumi na moja, kujumuisha na vijiji
vyake. 52 Arabu, Duma, Ehani, 53 Yanimu, Bethi Tapua, Afeka, 54 Humta, Kiriathi
Arba (ambayo ndio Hebroni), na Ziori. Hii ilikuwa miji tisa, pamoja na vijiji vyake.
55 Maoni, Karmeli, Zifu, Yuta, 56 Yezreeli, Yokdeamu, Zanoa, 57 Kaini, Gibea, na Timna.
Hii ilikuwa ni miji kumi, kujumuisha na vijiji vyake. 58 Halhuli, Bethi Zuri, Gedori,
59 Maarathi, Bethi Anothi, na Elitekoni. Hii ilikuwa miji sita, pamoja na vijiji vyake.
60 Kiriathi Baali (ambayo ndio Kiriathi Yearimu), na Raba. Hii ilikuwa ni miji miwili,
pamoja na vijiji vyake. 61 Katika nyika, kulikuwa na miji ya Bethi Araba, Midini,
Sekaka, 62 Nibushani, mji wa chumvi, na Eni Gedi. Hii ilikuwa miji, pamoja na vijiji
vyao. 63 Lakini kwa Wayebusi, wenyeji wa Yerusalemu, kabila la Yuda halikuweza
kuwafukuza, na hivyo, Wayebusi wanaishi pamoja na kabila la Yuda hadi leo hii.

# 16

1 Nchi waliyopewa kabila la Yusufu ilianzia katika Yordani huko Yeriko, mashariki
mwa chemichemi za Yeriko, kupitia nyikani, kupanda kutoka Yeriko kupitia nchi ya
milima ya Betheli. 2 Kisha uliendelea kutoka Betheli hadi Luzi na kupita hata Atarothi,
iliyo miliki ya Waarkiti. 3 Kisha ilishuka chini upande wa magharibi kuelekea himaya
ya Wayafuleti, hadi kufika miliki ya Loweri Bethi Horoni, na kisha iliendelea hadi
Gezeri; na ilikomea katika bahari. 4 Ilikuwa ni kwa njia hii makabila ya Yusufu,
yaani Manase na Efraimu yalipata urithi wao. 5 Eneo la kabila la Efraimu ambalo
lilikuwa limegawanya kwa koo zao lilikuwa kama ifuatavyo: mpaka wa urithi wao
katika upande wa mashariki ulikuwa Atarothi Ada uliopanda kuelekea Bethi Horoni
ya juu, 6 na kutoka pale uliendelea hadi katika bahari. Kutoka Mikimethathi katika
upande wa Kasikazini ulipinda upande wa mashariki kuelkea Taanathi Shilo na
kupita ng'ambo yake katika upande wa mashariki kukabili Yanoa. 7 Kisha ulishuka
kutoka Yanoa hadi Atarothi na hata Naara, na kisha ukafika Yeriko, na kuishia katika
Yordani. 8 Kutoka Tapua, mpaka uliendelea katika upande wa magharibi hata kijito
cha Kana na ulikomea katika bahari. Huu ulikuwa ni urithi wa kabila la Efraimu,
uliogawanywa katika koo zao, 9 pamoja na miji yao iliyochaguliwa kwa ajili ya kabila
la Efraimu iliyokuwa ndani ya urithi wa kabila la Manase - miji yote pamoja na
vijiji vyao. 10 Lakini hawakuwafukuza Wakanaani walioishi katika Gezeri, hivyo basi
Wakanaani wanaishi ndani ya Efraimu hadi leo, lakini watu hawa walifanywa kuwa
watumwa.

# 17

1 Na huu ndio mgao wa nchi kwa ajili ya kabila la Manase (aliyekuwa mzaliwa
wa kwanza wa Yusufu), ambayo ilikuwa kwa ajili ya Makiri, mzaliwa wa kwanza
wa Manase, ambaye alikuwa ni baba wa Gilieadi. Watoto wa Makiri walipewa nchi
ya Gileadi na Bashani, kwasababu Makiri alikuwa ni mtu wa vita. 2 Nchi iliyobaki

iligawiwa kwa kabila la Manase, walipewa kwa koo zao, ambazo ni Abi Ezeri, Heleki,
Asrieli, Shekemu, Heferi, na Shemida. Hawa walikuwa ni watoto wa kiume wa
Manase mwana wa Yusufu, waliwakilishwa na koo zao. 3 Basi Zelofehadi mwana wa
Heferi mwana wa Gileadi mwana wa Makiri mwana wa Manase hakuwa na watoto
wa kiume, bali alikuwa na watoto wa kike tu. Na majina ya binti zake yalikuwa
Mahila, Noa, Hogla, Milka na Tirsa. 4 Walimwendea Eliazeri kuhani, Yoshua mwana
wa Nuni, na viongozi na wakasema, “Yahweh alimwagiza Musa atupatie urithi wetu
pamoja na kaka zetu.” Hivyo, kwa kuzingatia agizo la Yahweh, aliwapa wanawake
hao urithi miongoni mwa ndugu za baba yao. 5 Manase alipewa sehemu kumi za nchi
katika Gileadi na Bashani, ambayo iko upande mwingine wa Yordani, 6 kwasababu ya
binti za Manase walipokea urithi pamona na watoto wake wa kiume. Nchi ya Gileadi
iligawanywa kwa kabila la Manase lililosalia. 7 Eneo la Manase lilianzia Asheri hadi
Mikimethathi, ambayo iko mashariki mwa Shekemu. Kisha mpaka ulienda upande
wa kusini kwa wale walioishi karibu na chemichemi ya Tapua. 8 ( Nchi ya Tapua
ilikuwa ni miliki ya Manase, lakini mji wa Tapua katika mpaka wa Manase ilikuwa ni
mali ya kabila la Efraimu.) 9 Kisha mpaka ulishuka kuelekea kijito cha Kana. Miji hii
kusini mwa kijito miongoni mwa miji ya Manase ilikuwa ni mali ya Efraimu. Mpaka
wa Manase ulikuwa upande wa kaskazini wa kijito, na ulikomea katika 10 bahari.
Na nchi iliyokuwa upande wa kusini ilikuwa ni ya Efraimu, na nchi iliyo upande
wa Kasikazini ilikuwa ni ya Manase; bahari ilikuwa ndoi mpaka. Kwa upande wa
kaskazini ulifika hata Asheri, na upande wa mashariki, Isakari. 11 Pia katika Isakari
na katika Asheri, Manase alimiliki Bethi Shani na vijiji vyake, Ibleamu na vijiji vyake,
wenyeji wa Dori na vijiji vyake, wenyeji wa Endori na vijiji vyake, wenyeji wa Taanaki
na vijiji vyake, na wenyeji wa Megido na vijiji vyake (na mji wa tatu ni Nafethi).
12 Lakini kabila la Manase halikuweza kuimiliki miji hiyo, kwa kuwa Wakanaani
waliendelea kuishi katika nchi hii. 13 Hata wakati watu wa Israeli walipopata nguvu
zaidi, hawakuwafukuzia mbali kabisa Wakanaani, bali waliwafanya kuwa watumwa.
14 Kisha wazawa wa Yusufu wakamwambia Yoshua, wakisema, “ Kwanini umetupa
mgao mmoja wa nchi na sehemu moja kwa ajili ya urithi, kwa kuwa tuko wengi, na
kwa muda wote Yahweh umetubaliriki? 15 Yoshua akawaambia, “Kama ninyi ni watu
wengi katika hesabu, pandeni ninyi wenyewe katika msitu na kuisafisha nchi kwa
ajili yenu wenyewe katika nchi ya Waperizi na ya Refaimu. Fanyeni hivi kwa kuwa
nchi ya milima ya Efraimu ni ndogo kwenu.” 16 Wazawa wa Yusufu wakasema, “Nchi
ya milima haitutoshi. Lakini Wakanaani wote wanaoishi katika bonde wana magari
ya chuma, wote walio katikaBethi Shani na vijiji vyake, na wale walio katika bonde
la Yezreeli.” 17 Kisha Yoshua akawaambi nyumba ya Yusufu, ambao ni Efraimu na
Manase, “ Ninyi ni watu mlio wengi katika hesabu, na mna nguvu kubwa. Hamtakiwi
kuwa na sehemu moja ya nchi mliogawiwa. 18 Nchi ya milima itakuwa yenu pia.
Ingawa ni msitu, mtaufyeka na kuimiliki hata mipaka yake ya mbali. Mtawafukuzia
mbali Wakanaani, ingawa wanayo magari ya chuma na ingawa pia wanazo nguvu.”

# 18

1 Kisha kusanyiko lote la watu wa Israeli walikusanyika pamoja hapo Shilo.
Walilijenga hema la kukutania hapo na waliishinda nchi mbele yao. 2 Kulikuwa na
makabila saba miongoni mwa watu wa Israeli ambayo yalikuwa bado hayajapewa
urithi wao. 3 Yoshua aliwaambia watu wa Israeli, “Je mtaacha mpaka lini katika
kuingia nchi ambayo Yahweh, Mungu wa baba zenu, amewapeni ninyi? 4 Chagueni
ninyi wenyewe watu watatu kutoka katika kila kabila, na nitawatuma. Wataenda na
kuipeleleza nchi juu na chini. Wataandika maelezo pamoja na maelekezo kuhusu
urithi wao, na kisha watarudi kwangu. 5 Wataigawanya nchi katika sehemu saba.

Yuda itasalia katika eneo lao upande wa kusini, na nyumba ya Yusufu itaendelea
katika himaya yao katika upande wa kaskazini. 6 Mtaigawanya nchi katika sehemu
saba na kisha mtaniletea maelezo hayo hapa kwangu. Nami nitapiga kura kwa ajili
yenu hapa mbele za Yahweh Mungu wetu. 7 Walawi hana sehemu miongoni mwenu,
kwa kuwa ukuhani wa Yahweh ni urithi wao. Makabila ya Gadi, Rubeni na nusu ya
kabila la Manase wameshapokea urithi wao ng'ambo ya Yordani. Huu ni urithi ambao
Musa mtumishi wa Yahweh aliwapa wao. 8 Hivyo, watu waliinuka na wakaenda.
Yoshua akawaamuru wale walioenda kuandika maelezo ya nchi, akisema, “Pandeni
juu na mshuke chini katika nchi na andikeni maelezo kuhusu nchi na kisha mrejee
kwangu. Nitapiga kura kwa ajili yenu hapa mbele za Yahweh huko Shilo. 9 Watu
walienda na walitembea juu na chini katika nchi na wakaandika maelezo kuihusu
nchi hiyo juu ya gombo kwa miji yake katika sehemu saba, kwa kutaja miji, kila
mmoja katika sehemu moja. Kisha wakarudi kwa Yoshua katika kambi huko Shilo.
10 Kisha Yoshua akapiga kura kwa ajili yao huko Shilo mbele za Yahweh. Na hapo
Yoshua akaigawa nchi kwa watu wa Israeli, kila kabila lilipewa sehemu ya nchi.
11 Katika kabila la Benyamini, ugawanaji wa nchi ulifanyika kwa kupewa kwa koo
zao. Eneo la nchi waliyopewa lilikuwa kati ya wazawa wa Yuda na wazawa wa
Yusufu. 12 Katika upande wa kusini, mpaka wao ulianzia katika Yordani. Mpaka
ulipanda hata sehemu ya juu kaskazini mwa Yeriko, na kisha ukapita katikati ya
nchi ya milima upande wa magharibi. Huko ukafika hadi nyika ya Bethi Aveni.
13 Kutoka hapo mpaka ulipita upande wa kusini katika mwelekeo wa Luzi (sehemu
ile ile inayoitwa Betheli). Kisha mpaka ukashuka chini hata Atarothi Adda, karibu
na mlima uliolekea kusini mwa Bethi Horoni. 14 Kisha mpaka ukaendelea upande
mwingine: katika upande wa magharibi uligeukia upande wa kusini, ulienda mbele
kuukabili mlima ulio ng'ambo ya Bethi Horoni. Mpaka huu ulikomea huko Kiriathi
Baali ( ambao ndio Kiriathi Yearimu), mji ambao ulikuwa ni wa kabila la Yuda. Na
huu ndio ulikuwa ni mpaka katika upande wa magharibi. 15 Katika upande wa kusini,
mpaka ulianzia nje tu ya Kiriathi Yearimu. Mpaka uliendelea kutoka Efroni hata
chemichemi ya maji ya Neftoa. 16 Kisha mpaka ulishuka chini hadi mpaka wa mlima
ambao ulikuwa mkabala ya bonde la Beni Hinomu, ambalo lililokuwa katika upande
wa kaskazini mwishoni mwa bonde la Refaimu. Kisha ulishuka chini kuelekea bonde
la Hinomu, sehemu ya kusini mwa mteremko wa Wayebusi, na uliendelea kushuka
chini hadi Eni Rogeli. 17 Ulizunguka upande wa kaskazini, kuelekea mwelekeo wa
Eni Shemeshi, na kutoka hapa ulienda hadi Gelilothi, ambao ulikuwa mkabala na
mwinuko wa Adumimu. Kisha ulishuka chini kuelekea Jiwe la Bohani mwana wa
Rubeni. 18 Ulipita kuelekea upande wa kaskazini wa bega la Bethi Araba na chini
kuelekea Araba. 19 Mpaka ulipita hadi upande wa bega la kaskazini la Bethi Hogla.
Mpaka ulikome katika ghuba ya kaskazini mwa Bahari ya Chumvi, katika upande
wa kusini mwishoni mwa Yordani. Huu ulikuwa ni mpaka wa upande wa kusini.
20 Yordani ulikuwa mpaka wake katika upande wa mashariki. Na huu ulikuwa ni
urithi wa kabila la Benyamini, na walipewa kwa kila ukoo wao, mpaka baada ya
mpaka, kwa kuizunguka nchi yote. 21 Kwa hiyo sasa miji ya kabila la Benyamini
kufuatana na koo zao ilikuwa ni Yeriko, 22 Bethi Hogla, Emeki Kezizi, Bethi Araba,
Zemaraimu, Betheli, 23 Avimu, Para, Ofra, 24 Kefari Amoni, Ofini, na Geba. Ilikuwa
ni miji kumi na miwili, pamoja na vijiji vyake. 25 Kulikuwa pia na miji ya Gibeoni,
Rama, Beerothi, 26 Mizpe, Kefira, Moza, 27 Rekemu, Iripeeli, Tarala, 28 Zela, Haelefu,
Yebusi (ambao ndio Yerusalemu), Gibea, na Kiriathi. Kulikuwa na miji kumi na nne,
pamoja na vijiji vyake. Huu ulikuwa ni urithi wa Benyamini kufuatana na koo zao.

# 19

[1] Upigaji wa pili wa kura uliangukia kwa Simoni na waligawiwa kwa kila ukoo
wao. Urithi wao ulikuwa katikati ya urithi ulikuwa ni mali ya kabila la Yuda. [2] Urithi
waliokuwa nao ni Beerisheba, Sheba, Molada, [3] Hazari Shuali, Bala, Ezemu, [4] Elitoladi,
Bethuli na Horma. [5] Simoni alikuwa pia na Ziklagi, Bethi Markabothi, Hazari Susa,
[6] Bethi Lebaothi, na Sharuheni. Kulikuwa na miji kumi na mitatu pamoja na vijiji
vyake. Vile vile [7] Simoni alimiliki Aini, Rimon, Etheri, na Ashani. Hii ilikuwa ni miji
minne pamoja na vijiji vyake. [8] Miji hii pamoja na vijiji vilivyoizunguka hata kufika
Baalathi Beeri (ambao ndio Rama katika Negevu). Huu ulikuwa ni urithi wa kabila
la Simoni, waliopewa kwa koo zao. [9] Urithi wa kabila la Simoni ulikuwa sehemu
ya himaya ya kabila la Yuda. Hii ni kwasababu nchi waliyopewa kabila la Yuda
ilikuwa ni kubwa kwao, na hivyo kabila la Simoni lilipokea urithi wao kutoka katika
sehemu yao ya katikati. [10] Upigaji wa kura ya tatu uliangukia kwa kabila la Zabuloni,
na walipewa kwa koo zao. Mpaka wa urithi wao ulianzia huko Saridi. [11] Mpaka
wao ulipanda upande wa magharibi kuelekea Marala na ukaigusa Dabeshethi, na
kisha ukasonga kuelekea kijito kilichokuwa mkabala na Yokineamu. [12] Kutoka Saridi
mpaka ulizunguka upande wa mashariki kuelekea mashariki na ulienda hadi mpaka
wa Kislothi Tabori. Kutoka hapo uliendelea hadi Daberathi na kisha ulipanda hata
Yafia. [13] Kutoka hapo ulipita katika upande wa mashariki mwa Gathi Heferi, na kisha
ukafika Ethikazini, baadaye ulienda hadi Rimoni na kisha ukageuka kuelekea Nea.
[14] Mpaka ulizunguka kueleka kaskazini ukafika Hanathoni na ulikomea katika bonde
la Ifta Eli. [15] Mkoa huu ulijumuisha miji ya Katathi, Nahalali, Shimroni, Idala, na
Bethlehemu. Kulikuwa na miji kumi na miwili, pamoja na vijiji vyake. [16] Huu ulikuwa
ni urithi wa kabila la Zabuloni, waliopewa kwa kufuatana na koo zao - miji pamoja na
vijiji vyake. [17] Upigaji kura wa nne uliangukia kwa Isakari, na waligawiwa kufuatana
na koo zao. [18] Eneo lao lilijumuisha Jezreelli, Kesuloothi, Shunemu, [19] Hafaraimu,
Shioni, na Anaharathi. [20] Pia ilijumuisha miji ya Rabithi, Kishioni, Ebezi, [21] Remethi,
Enganimu, Enihada, na Bethipazezi. [22] Mpaka wao ulifika Tabor, Shahazuma, na
Bethi Shemeshi, na ukakomea katika Yordani. Ilikuwa ni miji kumi na sita, pamoja na
vijiji vyake. [23] Huu ulikuwa ni urithi wa kabila la Isakari, na walipewa kufuatana na
koo zao - miji pamoja na vijiji vyake. [24] Upigaji wa kura ya tano uliangukia kwa kabila
la Asheri, na walipewa kwa koo zao. [25] Eneo lao lilijumuisha miji ya Helikathi, Hali,
Beteni, Akashafu, [26] Alameleki, Amadi, na Mshali. Mpaka wa magharibi ulitanuka
hadi Karmeli na Shihori Libnathi. [27] Kisha ulizunguka upande wa mashariki kueleka
Bethi Dagoni na ukaenda hadi Zabuloni, na kisha ukafika katika bonde la ifutaheli,
upande wa kaskazini mwa Bethemeki na Neieli. Baadaye uliendelea mbele hata
Kabuli kueleka upande wa Kaskazini. [28] Na kisha ulienda hadi Ebroni, Rehobu,
Hammoni, na Kana, hata kufika mji mkubwa wa Sidoni. [29] Mpaka ulirudi nyuma
kuelekea Rama, na kisha ukafika kwenye mji wa Tiro uliokuwa na ngome. Baada
ya hapo mpaka ulizunguka kuelekea Hosa na ulikomea katika bahari, katika mkoa
wa Akizibu, [30] Umma, Afeki, na Rehobu. Kulikuwa na miji ishirini na miwili, pamoja
na vijiji vyake. [31] Huu ulikuwa ni urithi wa kabila la Asheri, na waliopewa kwa koo
zao - miji pamoja na vijiji vyake. [32] Upigaji wa kura wa mara ya sita uliangukia kwa
kabila la Nafutali, na walipewa kufuatana na koo zao. [33] Mpaka wao ulianzia Helefu,
kutoka katika mwaloni huko Zaananimu, ulipanda hadi Adaminekebu na Yabneeli,
umbali kama Lakumu; na ulikomea katka Yordani. [34] Mpaka ule ulizunguka upande
wa magharibi kuelekea Aznothi Tabori na ulipanda hadi Hukoki; uligusa Zabuloni
katika upande wa kusini, na ulifika hata Asheri katika upande wa magharibi, na
Yuda katika upande wa mashariki huko katika mto Yordani. [35] Miji yenye ngome
ilikuwa ni Zidimu, Zeri, Hammathi, Rakathi, Kinnerethi, [36] Adama, Rama, Hazori,

[37] Kedeshi, Edrei, na Eni Hazori. [38] Pia kulikuwa na miji ya Yironi, Migdaleli, Horemu,
Bethi Anathi, na Bethi Shemeshi. Kulikuwa na miji kumi na tisa, pamoja na vijiji
vyake. [39] Huu ulikuwa ni urithi wa kabila la Nafutali, na walipewa miji pamoja
na vijiji vyake kufuatana na koo zao. [40] Upigaji wa kura ya saba uliangukia kwa
kabila la Dani, na walipewa kufuatana na koo zao. [41] Eneo lao la urithi lilijumuisha
miji ya Zora, Eshitaoli, Iri Shemeshi, [42] Shaalabini, Aijaloni, na Ithila. [43] Vile vile
lilijumuisha miji ya Eloni, Timna, Ekroni, [44] Eliteke, Gibethoni, Baalathi, [45] Yehudi,
Bene - Beraki, Gathi Rimoni, [46] Me -Yarkoni, na Rakoni sambamba na eneo la karibu
na Yopa. [47] Ilitokea wakati mpaka wa kabila la Dani ulipowapotea, kabila la Dani
waliishambulia Leshemu, wakapigana nao, na wakauteka. Waliua kila mtu kwa
upanga, wakauchukua ukawa mali yao, na wakakaa ndani yake. Wakauita mji ule
Dani jina la babu yao badala ya Leshemu. [48] Huu ulikuwa urithi wa kabila la Dani,
waliopewa kufuatana na koo zao - miji pamoja na vijiji vyake. [49] Walipomaliza
kugawana urithi wa nchi, watu wa Israeli walimpa urithi Yoshua mwana wa Nuni
kutoka miongoni mwao. [50] Kwa amri ya Yahweh walimpatia mji wa Timnathi Sera
ambao aliuomba, ulikuwa katika nchi ya milima ya Efraimu. Aliujenga mji na akaishi
huko. [51] Na huu ndio urithi ambao Eliazari kuhani, na Yoshua mwana wa Nuni, na
viongozi wa makabila ya familia za mababu zao miongoni mwa watu wa Israeli,
waligawa kwa kupiga kura huko Shilo, mbele za Yahweh katika mlango wa hema la
kukutania. Na hivyo wakamaliza kuigawa nchi.

# 20

[1] Baada ya hayo, Yahweh akamwambia Yoshua, [2] “Waambia watu wa Israeli,
na kusema, 'Chagueni miji ya makimbilio ambayo niliwaambia kupitia kwa Musa.
[3] Fanyeni hivi ili mtu akiua mtu bila kukusudia aweze kwenda huko. Miji hii itakuwa
ni sehemu ya kukimbilia kutoka kwa mtu yeyote yule anayetaka kulipiza kisasi kwa
damu ya mtu aliyeuliwa. [4] Atakimbilia kwa mji mmoja miongoni mwa miji hiyo na
atasimama mlangoni mwa lango la mji, na ataeleza kesi yake kwa wazee wa mji ule.
Kisha watamwingiza ndani ya mji na watampatia sehemu yake ya kuishi miongoni
mwao. [5] Na kama mtu akija akataka kulipiza kisasi kwa damu ya mtu yule ambaye
aliuliwa, ndipo watu wa mji hawatatakiwa kumtoa kwa wenye mamlaka mtu huyo
aliyeua. Hawaruhusiwi kufanya hivyo kwasababu alimwua jirani bila kukusudia
na hakuwa na chuki naye hapo awali. [6] Ni lazima akae katika mji ule mpaka pale
atakapokuwa amesimama mbele ya kusanyiko kwa ajili ya kuhukumiwa, hadi pale
atakapokufa mtu yule anayetumika katika nafasi ya kuhani mkuu katka siku hizo.
Na kisha mtu yule aliyeua bila kukusudia aweza kurudi nyumbani kwake, katika mji
ule ulikotoka. [7] Kwahiyo, Waisraeli wakaichaguia Kedeshi iliyoko Galilaya katika nchi
ya milima ya Nafutali, Shekemu katika nchi ya milima ya Efraimu, na Kiriathi Arba
(ambayo ndio Herbroni) katika nchi ya milima ya Yuda. [8] Katika ng'ambo ya Yordani
mashariki mwa Yeriko, walichagua mji wa Bezeri huko nyikani katika nyanda za
kabila la Rubeni; na Ramothi Gileadi kutoka kabila la Gadi; na Golani katika Bashani,
kutoka katika kabila la Manase. [9] Hii ni miji iliyochaguliwa kwa ajili ya watu wote
wa Israeli na kwa ajili ya wageni wanaoishi miongoni mwao, ili kwamba mtu yeyote
amwuaye mtu bila kukusudia aweza kukimbilia huko kwa ajili ya kupata usalama.
Mtu huyu hatakufa kwa mkono wa mtu yule anayetake kulipiza kisasi cha damu
iliyomwagwa, mpaka hapo kwanza mtuhumiwa atakaposimama mbele ya kusanyiko
la watu.

# 21

[1] Kisha wakuu wa koo za Walawi walimwendea Eliazari kuhani, na kwa Yoshua
mwana wa Nuni, na kwa viongozi wa familia za mababu zao miongoni mwa watu

wa Israeli. 2 Waliwaambia, “Yahweh aliwaagizeni ninyi kwa mkono wa Musa
kwamba mtupatieni miji ya kuishi yenye maeneo kwa ajili ya kuchungia ya mifugo.”
waliyasema haya huko Shilo katika nchi ya Kanaani. 3 Hivyo, kwa agizo la Yahweh,
watu wa Israeli waliwapa Walawi kutoka katika urithi wa wao miji ifuatayo pamoja
na maeneo yao ya kuchungia. 4 Upigaji wa kura kwa ajili ya koo za Wakohathi
ulileta matokeo haya: makuhani ambao ni wazawa wa Haruni ambao walitokana
na Walawi, walipokea miji kumi na mitatu waliopewa kutoka kwa kabila la Yuda,
kutoka kabila la Simoni, na kutoka kabila la Benyamini. 5 Koo zilizobaki za Wakohathi
walipokea kwa kupiga kura kwa miji kumi kutoka katika kabila za Efraimu, Dani, na
kutoka kwa nusu ya kabila la Manase. 6 Na watu wazawa wa Gershoni walipewa
miji kumi na mitatu kwa kupigiwa kura kutoka kwa koo za kabila la Isakari, Asheri,
Nafutali, na nusu ya kabila la Manase katika Bashani. 7 Watu waliokuwa wazawa wa
Merari walipokea miji kumi na miwili kutoka katika makabila ya Rubeni, Gadi na
Zabuloni. 8 Basi, watu wa Israeli waliwapa Walawi miji hii pamoja na maeneo yao ya
kuchungia, kwa kupiga kura, kama vile Yahweh alivyokuwa ameagiza kwa mkono wa
Musa. 9 Kutoka kwa makabila la Yuda na Simoni, waliwapa nchi katika miji ifuatayo
iliyoorodheshwa kwa majina. 10 Miji hii walipewa wazawa wa Haruni, ambao
walikuwa miongoni mwa koo za Wakohathi, ambao walitoka katika kabila la Lawi.
Kwa kuwa upigaji wa kura ya kwanza uliwaangukiwa wao. 11 Waisraeli waliwapatia
Kiriathi Arba ( Arba alikuwa ni baba wa Anaki), eneo hilo liliitwa pia Hebroni, katika
nchi ya milima ya Yuda, pamoja na maeneo ya kulishia mifugo yaliyouzunguka
mji. 12 Lakini mashamba ya mji na vijiji vyake vilikuwa tayari ameshapewa Kalebu
mwana Yefune, kama mali yake. 13 Na kwa wana wa Haruni kuhani, waliwapa
Hebroni pamoja na eneo lake la kulishia mifugo ambao ulikuwa ni mji wa makimbilio
kwa mtu aliyeua mtu bila kukusudia na Libna pamoja na maeneo ya kulishia mifugo.
14 Na Yatiri pamoaja na maeno yake ya kuchungia, na Eshitemoa pamoja na maeneo
yake ya malisho. 15 Lakini pia waliwapa Holoni pamoja na maeneo yake ya malisho,
Debiri pamoja na maeneo yake ya malisho, 16 Aini pampoja na maeneo yake ya
malisho, na Bethi Shemeshi pamoja na maeneo yake ya malisho. Ilikuwa ni miji
kumi na tisa ambayo walipewa kutoka katika makabila haya mawilil. 17 Kutoka
katika kabilala Benyamini walipewa Gibea pamoja na maeneo yake ya malisho, na
Geba pamoja na maeneo yake ya malisho, 18 na Anathothi pamoja na maeneo yake ya
malisho, na amoni pamoja na vitongoji vyake vinne. 19 Miji waliyopewa makuhani,
wana wa Haruni, ilikuwa ni miji kumi na mitatu kwa ujumla, kujumlisha na maeneo
yake ya malisho. 20 Na kwa ajili ya sehemu ya familia ya Kohathi iliyosalia, wale
Walawi walio wa familia ya Kohathi, walipewa miji kutoka katika kabila la Efraimu
kwa kupiga kura. 21 Walipewa Shekemu pamoja na maeneo yake ya malisho katika
nchi ya milima ya Efraimu - mji wa makimbilio kwa mtu aliyeua mtu bila kukusudia,
na Gezeri pamoja na maeneo yake ya malisho, 22 na Kibzaimu pamoja na maeneo
yake ya malisho, na Bethi Horoni pamoja na maeneo yake ya malisho, ilikuwa miji
minne kwa ujumla wake. 23 Kutoka katika kabila la Dani, ukoo wa Kohathi ulipewa
Elteke pamoja na maeneo yake ya malisho, na Gibethoni pamoja na maeneo yake ya
malisho, na 24 Aijaloni pamoja na maeneo yake ya malisho, na Gathrimoni pamoja na
maeneo yake ya malisho, ilikuwa ni miji minne kwa ujumla wake. 25 Kutoka katika
nusu ya kabila la Manase, ukoo wa Kohathi walipewa miji miwili - Taanaki pamoja
na maeneo yake ya malisho na Gathirimoni pamoja na maeneo yake ya malisho.
26 Kulikuwa na miji kumi kwa ujumla wake kwa ajili ya koo zilizosalia za Wakohathi,
pamoja na maeneo yao ya malisho. 27 Kutoka katika nusu ya kabila la Manase, jamaa
za Gershoni, ambazo hizi zilikuwa ni koo zingine za Walawi, zilipewa Golani katika
Bashani pamoja na maeneo yao ya malisho, ni mji wa makimbilio kwa ajili ya mtu

yeyote aliyeua mtu bila kukusudia, sambamba na Beeshitera pamoja na maeneo yake
ya malisho - ilikuwa miji miwili kwa ujumla. 28 Koo za Gershoni zilipewa pia miji
minne kutoka kwa kabila la Isakari - Kishoni sambamba na maeneo yake ya malisho,
Daberathi pamoja na maeneo yake ya malisho, 29 Yarmuthi pamoja na maeneo yake
ya malisho, na Engnimu pamoja na maeneo yake ya malisho. 30 Kutoka katika kabila
la Asheri, walipewa miji minne kwa ujumla - Mishali pamoja na maeneo yake ya
malisho, Abdoni pamoja na maeneo yake ya malisho, 31 Helikathi pamoja na maeneo
yake ya malisho, na Rehobu pamoja na maeneo yake ya malisho. 32 Kutoka kwa
kabila la Nafutali, nasaba za Gershoni walipewa miji mitatu kwa ujumla - Kedeshi
katika Galilaya pamoja na maeneo yake ya malisho, ulikuwa ni mji wa makimbilio
kwa mtu yeyote aliyeua mtu bila kukusudia; na Hamothidori pamoja na maeneo
yake ya malisho, na Kartani pamoja na maeneo yake ya malisho. 33 Kulikuwa na miji
kumi na mitatu kwa ujumla, kujumuisha na maeneo yake ya malisho, kwa ajili ya
koo za Gershoni. 34 Na kwa Walawi waliosalia, koo za Merari waliokuwa wamepewa
kutoka katika kabila la Zabuloni: Yokneamu pamoa na maeneo yake ya marisho,
Karta pamoja na maeneo yake ya malisho, 35 Dimna pamoja na maeneo yake ya
malisho, na Nahalali pamoja na maeneo yake ya malisho- ilikuwa ni miji minne
kwa ujumla. 36 Kwa mbari za Merari walipewa miji minne kutoka katika kabila
la Rubeni: Bezeri pamoja na maeneo yake ya malisho, Yahazi pamoja na maene
yake ya malisho, 37 na Kedemothi pamoja na maeneo yake ya malisho, na Mefaathi
pamoja na maeneo yake ya malisho. 38 Kutoka katika kabila la Gadi walipewa miji
ya Ramothi katika Gileadi pamoja na sehemu zake za malisho - huu ulikuwa ni mji
wa makimbilio kwa mtu aliyeua mtu mwenzake bila kukusudia - na Mahanaimu
pamoja na sehemu zake za malisho. 39 Koo za Merari zilipewa pia Heshiboni pamoja
na maeneo yake ya malisho, na Yazeri pamoja na malisho yake. 40 Hii ilikuwa ni
miji minne kwa ujumla wake. Hii yote ilikuwa ni miji ya koo kadhaa za Merari,
ambao walitoka katika kabila la Lawi, miji kumi na miwili walipewa wao kwa kupiga
kura. 41 Miji waliyopewa Walawi kutoka katikati ya nchi iliyomilikiwa na watu wa
Israeli ilikuwa miji arobaini na nane, kujumuisha na sehemu za malisho yao. 42 Miji
hii kila mmoja ulikuwa na maeneo yake ya malisho kwa kuuzunguka mji. Miji hii
yote ilikuwa hivyo. 43 Basi Yahweh aliwapa Israeli nchi yote ambayo aliwaapia baba
zao kuwa atawapa. Waisraeli waliimiliki nchi na wakakaa humo. 44 Kisha Yahweh
akawapa pumziko kwa kila upande, kama tu alivyowaahidia baba zao. Hakuna
hata adui mmoja atakayeweza kuwashinda. Yawhew aliwatia maadui wao wote
mikononi mwao. 45 Hakuna hata kitu kimoja miongoni kwa ahadi nzuri ambazo
Yahweh alizisema kwa nyumba ya Israeli ambazo hazikutimia. Ahadi zote zilitimia.

## 22

1 Kwa wakati huo, Yoshua aliwaita Warubeni, Wagadi, na nusu ya kabila la Manase.
2 Aliwaambia, "Mmefanya kila kitu ambacho Musa mtumishi wa Yahweh aliwaagiza
ninyi. Mmeitii sauti yangu katika yote niliyowaagiza. 3 Bado hamjawaacha ndugu
zenu hawa kwa siku zote hizi, mpaka siku hii ya leo. Na mmetimiza wajibu
unaotakiwa na amri za Yahweh Mungu wenu. 4 Sasa Yahweh Mungu wenu amewapa
pumziko ndugu zenu, kama alivyowaahidi. Hivyo basi, rudini na mwende katika
hema zenu katika nchi mnayoimiliki, ambayo Musa mtumishi wa Yahweh aliwapeni
katika upande mwingine wa Yordani. 5 Lakini zingatieni kuzishika amri na sheria
ambazo Musa mtumishi wa Yahweh aliwaagiza ninyi, kumpenda Yahweh Mungu
wenu, kutembea katika njia zake, kuzitunza amri zake, na kuambatana naye na
kumwabudu yeye kwa moyo wenu wote na kwa roho zenu zote. 6 Basi Yoshua
akawabariki na kisha akawaacha waende zao, nao wakarudi katika hema zao. 7 Na

kwa nusu ya kabila la Manase, Musa alikuwa amewapa urithi katika Bashani, lakini
kwa nusu ya kabila hilo, Yoshua aliwapa urithi karibu na ndugu zao katika nchi
magharibi mwa Yordani. Yoshua aliwaaga waende katika hema zao; aliwabarikia,
8 na kisha akawaambia, “Rudini katika hema zenu mkiwa na pesa nyingi, na mkiwa
na mifugo mingi, pamoja na na fedha, na dhahabu, na shaba na chuma, na nguo
nyingi. Gawaneni na ndugu zenu nyara mlizochukua kutoka kwa maadui zenu.
9 Hivyo, wazawa wa Rubeni, wazawa wa Gadi na nusu ya kabila la Manase walirudi
nyumbani, waliwaacha watu wa Isaeli hapo Shilo, ambayo imo ndani ya nchi ya
Kanaani. Waliondoka wakaenda katika mkoa wa Gileadi, katika nchi yao, ambayo
wao wenyewe waliimiliki, katika utiifu wa amri za Yahweh, kwa mkono wa Musa.
10 Nao walipofika hapo Yordani iliyo katika nchi ya Kanaani, Warubeni na Wagadi
na nusu ya kabila la Manase walijenga madhabahu karibu na Yordani, madhabahu
kubwa na iliyotokeza na mashuhuri. 11 Watu wa Israeli walisikia habari hizo na
wakaseam, “Tazama! Watu wa Rubeni, Gadi na nusu ya kabila la Manase wamejenga
madhabahu mbele ya nchi ya Kanaani, huko Gelilothi, katika mkoa karibu na Yordani,
katika upande ambao ni miliki ya watu wa Israeli.” 12 Wakati watu wa Israeli
waliposikia hivyo, kusanyiko lote la watu wa Israeli walikusanyika kwa pamoja huko
Shilo ili wapande kupigana vita nao. 13 Kisha watu wa Israeli walituma wajumbe kwa
Warubeni, Wagadi na nusu ya kabila la Manase, katika nchi ya Gileadi. Walimtuma
pia Finehasi mwana wa Eliezari, kuhani, 14 na viongozi kumi pamoja naye, mmoja
kutoka katika familia za mababa wa Israeli, na kila mmoja wao alikuwa ni kiongozi
wa ukoo miongoni mwa watu wa Israeli. 15 Walienda kwa watu wa Rubeni, Gadi, na
nusu ya kabila la Manase, katika nchi ya Gileadi, na wakawaambia: 16 “Kusanyiko lote
la Yahweh linasema kuwa, ' Ni jambo gani hili lisilo la uaminifu ambalo mmelitenda
kinyume na Mungu wa Israeli, kwa kugeuka badala ya kumfuata Yahweh siku hii
na kujijengea wenyewe madhabahu katika uasi kinyume na Yahweh katika siku hii?
17 Je dhambi zetu huko Peori hazikututosha? Bado hata sasa hatujajitakasa wenyewe
kwa dhambi hiyo. Kwa ajili ya dhambi ile lilikuja pigo kwa kusanyiko lote la Yahweh.
18 Je, nanyi leo pia mwageuka na kuacha kumfuata Yahweh? Kama mtaasi kinyume
na Yahweh leo, kesho atakuwa na hasira na kusanyiko lote la Israeli. 19 Na kama
nchi ambayo mnaimiliki imetiwa unajisi, basi mwaweza kuvuka katika nchi ambayo
Sanduku la Yahweh lasimama na mjichukulie kwa ajili yenu umiliki miongoni mwetu.
Hamtakiwi kuasi kinyume na Yahweh tu, wala kuasi kinyume chetu kwa kujenga
madhabahu kwa ajili yenu wenyewe badala ya madhabahu ya Yahweh Mungu wa
wetu. 20 Je hakuwa Akani mwana wa Zera aliyeivunja imani kwa vitu vile ambavyo
vilikuwa vimetunzwa kwa ajili ya Mungu? Na je ghadhabu ya Mungu haikushuka
kwa watu wote wa Israeli? Mtu yule hakuangamia peke yake kwa uovu wake. 21 Kisha
makabila ya Rubeni, Gadi na nusu ya kabila la Manase wakawajibu wazee wa koo za
Israeli: 22 “Yahweh, Mungu Mwenye nguvu! Yahweh, Mungu Mwenye nguvu! Yeye
anajua, na Israeli naijue yenyewe! Kama ilikuwa ni katika uasi au katika kuvunja
imani kinyume na Yahweh, msituache hai katika siku hii ya leo 23 kwa ajili ya kujenga
madhabahu ili tugeuka na kuacha kumfuata Yahweh. Kama tumejenga madhabahu
hii ili kutoa juu yake sadaka ya kuteketezwa, sadaka ya nafaka, au sadaka ya amani,
basi Yahweh na atuadhibu. 24 La hasha, tulifanya hivyo kwa sababu ya hofu kwamba
katika siku zijazo watoto wenu wanaweza kuwaambia watoto wetu, ' Mna nini ninyi
na Yahweh, Mungu wa Israeli? 25 Kwa kuwa Yahweh ameifanya Yordani kuwa mpaka
kati yetu na ninyi. Ninyi watu wa Rubeni na watu wa Gadi, hamna kitu chochote
naYahweh.' Na kwa hali hiyo, watoto wenu wanaweza kuwafanya watoto wetu
waacha kumwabudu Yahweh. 26 Basi tukasema, 'Hebu na tujenge sasa madhabahu,
si kwa ajili ya sadaka ya kuteketezwa wala si kwa sadaka yoyote ile, 27 ila iwe ni

ushahidi kati yetu na ninyi, na kati ya kizazi chetu baada yetu, kwamba tutafanya
ibada ya Yahweh mbele yake, pamoja na sadaka zetu za kuteketezwa na dhabihu zetu
na sadaka zetu za amani, ili kwamba watoto wenu wasiweze kuwaambia watoto wetu
katika siku zijazo kuwa, “Hamna sehemu katika Yahweh.”' [28] Hivyo tukasema, 'kama
hili litasemwa kwa kwetu au kwa watoto wetu katika siku zijazo, tutasema, “ Tazama!
Huu ni mfano wa madhabahu ya Yahweh, ambayo mababu zetu waliifanya, si kwa
ajili ya sadaka za kuteketezwa, wala si kwa dhabihu, bali kwa ajili ya ushahidi kati
yetu ninyi.” [29] Na iwe mbali nasi kwamba tunataka kugeuka kinyume na Yahweh,
na kuacha kumfuata yeye kwa kujenga madhabahu kwa ajili sadaka ya kuteketezwa,
na kwa sadaka ya nafaka, au kwa dhabihu, badala ya madhabahu ya Yahweh Mungu
wetu ambayo iko mbele ya hema la kukutania.'” [30] Finehasi kuhani na viongozi
wa watu, ambao ni wakuu wa koo za Waisraeli ambao walikuwa pamoja naye,
waliposikia maneno amabayo watu wa Rubeni, Gadi na nusu ya kabila la Manase,
kwamba yalikuwa ni mazuri machoni pao. [31] Finehasi mwana wa Eliazeri kuhani
aliwaambia watu wa Rubeni, Gadi na Manase, “Leo tumejua kwambaYahweh yuko
miongoni mwetu, kwa kuwa hamjatenda uvunjaji wa imani kinyume naye. Sasa,
mmewaokoa watu wa Israeli kutoka katika mkono wa Yahweh.” [32] Kisha Finehasi
mwana wa Eliazeri kuhani, na viongozi walirudi kutoka kwa Warubeni na Wagadi,
kutoka katika nchi ya Gileadi, na kurudi katika nchi ya Kanaani, kwa watu wa Israeli,
na waliwaletea taarifa. [33] Taarifa yao ilikuwa nzuri katika macho ya watu wa Israeli.
Watu wa Israeli walimbarikia Mungu na hawakuendelea kusema tena juu ya kuinua
vita dhidi ya Warubeni na Wagadi, ili kuiharibu nchi ambayo walikuwa wanaishi.
[34] Warubeni na Wagadi waliita ile madhabahu “Ushahidi,” kwa kuwa walisema, “Ni
ushahidi miongoni mwetu kuwa Yahweh ni Mungu.”

# 23

[1] Na baada ya siku nyingi, kipindi ambacho Yahweh alikuwa ameipa Israeli
pumziko kutoka maadui zao waliowazunguka, [2] Joshua alikuwa mzee sana. Yoshua
aliwaita Waisraeli wote, na wazee wao, na viongozi, na waamuzi, na kwa maafisa, na
kisha akawaambia, “Mimi nimezeeka sana. [3] Mmeshaona kila kitu ambacho Yahweh
Mungu wenu ameshafanya kwa mataifa haya yote kwa ajili yenu, kwa kuwa ni
Yahweh Mungu wenu ambaye amewapigania ninyi. [4] Tazama! Nimeshawakabidhi
kwenu mataifa yaliyosalia ili kuyateka kwa ajili ya kupata urithi ya makabila yenu,
sambasamba na mataifa yote ambayo tayari nimeshayaangamiza, tangu Yordani
hadi Bahari kuu katika upande wa magharibi. [5] Yahweh Mungu wenu atayaondoa.
Atayafukuzia mbali kutoka kwenu. Ataiteka nchi yao, nanyi mtaimiliki nchi yao,
kama vile Yahweh Mungu wenu alivyowaahidi ninyi. [6] Hivyo, iweni jasiri, ili kwamba
mtunze na kuyafanya yale yote yaliyoandikwa katika kitabu cha sheria ya Musa,
msikengeuke upande wa kulia wala upande wa kushoto, [7] basi msichanganyikane
na mataifa haya ambayo yamesalia miongoni mwenu, wala msiyataje majina ya
miungu yao, wala msiape kwayo, wala msiiabudu, wala msiipigie magoti. [8] Badala
yake, mnatakiwa kumshika sana Yahweh Mungu wenu kama vile mlivyofanya siku
hii ya leo. [9] Kwa kuwa Yahweh ameyafukuzia mbali mbele yenu mataifa makubwa
yenye nguvu. Hakuna hata mmoja aliyeweza kusimama mbele yenu hata siku hii ya
leo. [10] Mtu yeyote mmoja wa kwenu atawafanya watu elfu wakimbie mbali, kwa
kuwa Yahweh Mungu wenu, ndiye anayepigania ninyi, kama vile alivyowaahidi.
[11] Zingatieni kwa uangalifu ili mmpende Yahweh Mungu wenu. [12] Lakini kama
mkiegeuka na kushikamana na watu walioalia wa mataifa haya waliobaki miongoni
mwenu, au kuoana nao, au kama mkishirikiana pamoja nao, na wao pamoja nanyi,
[13] jueni kwa hakika kwamba Yahweh Mungu wenu hatayafukuzia mbali mataifa haya

yatoke kati yenu. Badala yake, watakuwa kitanzi na mtego kwenu, viboko migongoni
mwenu na miiba machoni mwenu, mpaka pale mtakapoangamia katika nchi hii nzuri
ambayo Yahweh Mungu wenu amewapeni ninyi. 14 Na sasa ninaenda katika njia ya
dunia yote, na mnajua kwa moyo na roho zenu zote kwamba hakuna hata neno
moja ambalo halijatimia kati ya mambo yote mazuri ambayo Yahweh Mungu wenu
aliyaahidi juu yenu. Vitu hivi vyote vimetokea kwa ajili yenu. Hakuna hata moja
lililoshindikana. 15 Lakini kama kila neno ambalo Yahweh Mungu wenu alilowaahidi
limekwisha kutimia, hivyo Yahweh atawaletea juu yenu mabaya yote mpaka pale
atakapokuwa amewaangamiza katika nchi hii nzuri ambayo Yahweh Mungu wenu
amewapeni ninyi. 16 Atafanya hivi kama mtalivunja agano la Yahweh Mungu wenu,
ambalo aliwaagizeni kulitunza. Kama mtaenda na kuiabudu miungu mingine na
kuiinamia, ndipo hasira ya Yahweh itawaka kinyume nanyi, na ninyi mtaangamia
upesi katika nchi nzuri ambayo amekwisha kuwapeni ninyi."

# 24

1 Kisha Yoshua aliyakusanya pamoja makabila yote ya Israeli huko Shekemu na
aliwaita wazee wa Israeli, viongozi, waamuzi na maafisa wao, nao wakajihudhurisha
mbele za Mungu. 2 Yoshua akawaambia watu wote, "Hiki ndicho Yahweh, Mungu
wa Israeli anachokisema, 'Mababu zenu kwa miaka mingi iliyopita waliishi ng'ambo
ya mto Frati - Tera, baba wa Ibrahimu na baba wa Nahori - nao waliabudu miungu
mingine. 3 Lakini nilimchukua baba yenu kutoka ng'ambo ya Frati na nikamwongoza
mpaka katika nchi ya Kanaani, na nilimpa watoto wengi kupitia kwa Isaka mwanaye.
4 Na Isaka nikampa Yakobo na Esau. Nilimpa Esau nchi ya milima ya Seiri ili aimiliki,
lakini Yakobo na watoto wake walishuka kwenda Misri. 5 Nilimtuma Musa na Haruni,
na niliwapiga Wamisri kwa mapigo. Baada ya hapo, niliwatoa ninyi. 6 Niliwatoa baba
zenu nje ya nchi ya Misri, nanyi mkafika hata katika bahari. Wamisri waliwafuata
kwa magari na wapanda farasi hata katika bahari ya matete. 7 Na baba zenu
walipomwita Yahweh, aliweka giza kati yenu na Wamisri. Aliileta bahari ije juu yao
na kuwafunika. Mliona yale niliyoyakifanya huko Misri. Kisha mliishi jangwaani kwa
muda mrefu. 8 Niliwaleta katika nchi wa Waamori, ambao waliishi katika upande
mwingine mwa Yordani. Walipigana nanyi, nami niliwatia katika mkono wenu.
Mliimiliki nchi yao, nami niliwaangamiza mbele yenu. 9 Kisha Balaki mwana wa
Zipori, mfalme wa Moabu, aliinuka na kuishambulia Israeli. Alimwita na kumtuma
Baalamu mwana wa Beori, ili kuwalaani ninyi. 10 Lakini sikumsikiliza Balaamu. Kwa
hakika, aliwabarikia ninyi. Basi, niliwaokoa na mkono wake. 11 Mlivuka Yordani na
mkafika Yeriko. Viongozi wa Yeriko waliinuka wapigane nanyi, pamoja na Waamori,
Waperizi, Wakanaani, Wahiti, Wagirgashi, Wahivi na Wayebusi. Niliwapa ninyi
ushindi dhidi yao na niliwaweka chini ya mamlaka yenu. 12 Nilituma manyingu
mbele yenu, ambayo yaliwafukuzia mbali na wafalme wawili wa Waamori watoke
mbele yenu. Haikutokea kwa sababu ya upanga wenu wala kwa upinde wenu.
13 Niliwapeni ninyi nchi ambayo hamkuifanyia kazi na miji ambayo hamkuijenga,
na sasa mnaishi ndani yake. Mnakula matunda ya mizabibu na na mashamba ya
mizeituni ambayo hamkuyapanda'. 14 Basi sasa mcheni Yahweh na kumwabudu yeye
kwa uadilifu na uaminifu wote; jitengeni na miungu ambayo baba zenu waliiabudu
ng'ambo ya Frati na katika Misri, na mkamwabudu Yahweh. 15 Na kama inaonekana
kuwa ni vibaya machoni penu kumwabudu Yahweh, chagueni ninyi katika siku hii
ya leo ni nani mtakayemtumikia, kama ni miungu ambayo baba zenu waliiabudu
ng'ambo ya Frati, au miungu ya Waamori, ambao ninyi mnakaa ndani ya nchi yao.
Lakini kwangu mimi na nyumba yangu, tutumwabudu Yahweh." 16 Watu walijibu
na kusema, "Hatutaweza kumwacha Yahweh na kuitumikia miungu mingine, 17 kwa

kuwa ni Yahweh Mungu wetu ambaye alitutoa sisi na baba zetu kutoka katika nchi ya
Misri, katika nyumba ya utumwa, na ambaye alifanya hizo ishara kubwa mbele yetu,
na ambaye alituhifadhi sisi katika njia zote ambazo sisi tuliziendea, na miongoni
mwa mataifa yote ambayo tulipita kati kati yake, 18 Na Yahweh aliwaondoa mbele
yetu watu wote, na Waamori walioishi katika nchi hii. Hivyo, tutamwabudu Yahweh
pia, kwa kuwa ni Mungu wetu" 19 Lakini Yoshua akawaambia watu, "Hamwezi
kumtumikia Yahweh, kwa kuwa ni Mungu mtakatifu; ni Mungu mwenye wivu;
hatawasamehe makosa na dhambi zenu. 20 Kama mtamwacha Yahweh na kuabudu
miungu ya kigeni, basi atageuka na kuwaharibu. Atawaangamizeni baada ya kuwa
amewatendea mema." 21 Lakini watu walimwambia Yoshua, "Hapana, tutamwabudu
Yahweh." 22 Kisha Yoshua akawaambia watu, "Ninyi ni mashahidi dhidi yenu
wenyewe kuwa mmemchagua Yahweh ninyi wenyewe, ili mmwabudu yeye." Watu
walijibu, "Sisi ni mashahidi." 23 "Sasa wekeni mbali miungu ya kigeni iliyoko
kwenu, na geuzeni moyo wenu umwelekee Yahweh, Mungu wa Israeli." 24 Watu
wakamwambia Yoshua, "Tutamwabudu Yahweh Mungu wetu. Tutaisikiliza sauti
yake. 25 Yoshua alifanya agano na watu siku hiyo. Aliziweka maagizo na sheria huko
Shekemu. 26 Yoshua aliyaandika maneno haya katika kitabu cha sheria za Mungu.
Alichukua jiwe kubwa na kulisimamisha hapo chini ya mti wa mwaloni uliokuwa
karibu na mahali pa takatifu pa Yahweh. 27 Yoshua akawaambia watu, "Tazama,
jiwe hili litakuwa ushuhuda dhidi yenu. Limeyasikia maneno yote ambayo Yahweh
alitwambia. Hivyo, litakuwa ni shahidi dhidi yenu, hamtakiwi kumkana Mungu
wenu." 28 Basi Yoshua aliwaacha watu waende zao, kila mmoja aliende kwenye urithi
wake. 29 Baada ya mambo haya, Yoshua mwana wa Nuni, mtumishi wa Yahweh,
alikufa akiwa na miaka 110. 30 Walimzika katika mpaka wa urithi wake mwenyewe
huko Timnathi Sera, ambayo iko kwenye nchi ya milima ya Efraimu, upande wa
Mlima Gaashi. 31 Israeli ilimwabudu Yahweh siku zote za maisha ya Yoshua, na siku
zote za wazee ambao walidumu pamoja na Yoshua, wale ambao waliona kila kitu
ambacho Yahweh alikuwa ameifanyia Israeli. 32 Mifupa ya Yusufu ambayo watu
wa Israeli waliileta kutoka Misri, waliizika huko shekemu, katika sehemu ya nchi
ambayo Yakobo alikuwa ameinunua kutoka kwa wana wa Hamori, baba wa Shekemu.
Aliinunua kwa vipande mia moja vya fedha, na ulikuwa urithi kwa wazawa wa
Yusufu. 33 Eliazeri mwana wa Haruni alikufa pia. Walimzika huko Gibea, katika mji
wa ambao alikuwa amepewa Finehasi mwanaye, na ulikuwa katika nchi ya milima
ya Efraimu.

# Waamuzi

1 Baada ya kifo cha Yoshua, wana wa Israeli walimuuliza Yahweh wakisema, “Ni
nani atawashambulia kwanza Wakanaani kwa ajili yetu, ili kupigana nao? 2 Yahweh
akasema, “Yuda atawashambulia. Tazama, nimewapa kumiliki nchi hii. 3 Watu
wa Yuda wakawaambia wana wa Simeoni, ndugu zao, “Njoo pamoja nasi katika
eneo letu ambalo tumepewa ili kwa pamoja tupigane na Wakanaani. Na sisi pia
tutakwenda nanyi katika eneo mlilopewa.” Basi kabila la Simeoni wakaenda pamoja
nao. 4 Watu wa Yuda wakashinda, na Bwana akawapa ushindi juu ya Wakanaani
na Waperizi. Wakawaua watu elfu kumi huko Bezeki. 5 Wakamkuta Adoni Bezeki
huko Bezeki, nao wakapigana naye na kuwashinda Wakanaani na Waperizi. 6 Lakini
Adoni Bezeki akamkimbilia, wakamfuata na kumshika, nao wakavikata vidole gumba
na vidole vyake vikubwa. 7 Adoni Bezek akasema, “Wafalme sabini, ambao na
vidole gumba vyako na vidole vikubwa vilivyokatwa, walikusanya chakula chao
chini ya meza yangu. Kama nilivyofanya, hata hivyo Mungu amefanya kwangu.”
Wakamleta Yerusalemu, naye akafa huko. 8 Watu wa Yuda wakapigana dhidi ya jiji
la Yerusalemu na kulichukua. Walishambulia kwa makali ya upanga na wakauwasha
mji kwa moto. 9 Baada ya hayo, watu wa Yuda walikwenda kupigana na Wakanaani
waliokaa mlimani, Negebu, na magharibi mwa milima. 10 Yuda akaenda dhidi ya
Wakanaani waliokaa Hebroni (jina la Hebroni hapo awali ilikuwa Kiriath-arba), nao
wakamshinda Sheshai, Ahimani na Talmai. 11 Kutoka huko watu wa Yuda walipigana
na wenyeji wa Debiri (jina la Debiri hapo awali ilikuwa Kiriath-seferi). 12 Kalebu
akasema, Yeyote atakayeivamia Kiriath-seferi na kuichukua, nitampa Aksa, binti
yangu, awe mkewe. 13 Otinieli, mwana wa Kenazi, ndugu mdogo wa Kalebu, akaiteka
Debiri, naye Kalebu akampa Aksa, binti yake, awe mkewe. 14 Ndipo Aksa alifika kwa
Othnieli, naye akamsihi amuombe baba yake ampe shamba. Alipokuwa akishuka
katika punda wake, Kalebu akamwuliza, “Nikufanyie nini?” 15 Akamwambia,
Nibariki. Kwa kuwa umenipa nchi ya Negebu, nipe pia chemchemi za maji. Kwa
hiyo Kalebu akampa chemchemi za juu na chemchemi za chini. 16 Kizazi cha Mkeeni
shemeji yake na Musa, walikwenda kutoka mji wa Mitende pamoja na watu wa Yuda,
mpaka jangwa la Yuda, ambalo liko Negevu, kuishi na watu wa Yuda karibu na
Arad. 17 Nao watu wa Yuda wakaenda pamoja na wana wa Simeoni ndugu zao,
wakawaangamiza Wakanaani waliokaa Zefathi, wakaiharibu kabisa. Mji uliitwa
Horma. 18 Watu wa Yuda pia waliiteka Gaza na nchi iliyoizunguka, Ashkeloni na
nchi iliyoizunguka, na Ekron na nchi iliyoizunguka. 19 Yahweh alikuwa pamoja na
watu wa Yuda na wakaimiliki nchi ya milima, lakini hawakuweza kuwatoa wenyeji
wa kwenye bonde kwa sababu walikuwa na magari ya chuma. 20 Hebroni alipewa
Kalebu (kama Musa alivyosema), naye akawafukuza kutoka huko wana watatu
wa Anaki. 21 Lakini wana wa Benyamini hawakuwafukuza Wayebusi waliokaa
Yerusalemu. Basi Wayebusi wakakaa na watu wa Benyamini huko Yerusalemu
hata leo. 22 Nyumba ya Yusufu ilijiandaa kuishambulia Betheli, na Yahweh alikuwa
pamoja nao. 23 Walipeleka watu kuipeleleza Betheli (jiji lililoitwa Luzu). 24 Wapelelezi
waliona mtu akitoka nje ya jiji, wakamwambia, “Tafadhali tuonyeshe jinsi ya kuingia
ndani ya jiji, na tutakutendea mema.” 25 Aliwaonyesha njia ya kuingia kwenye mji.
Waliuteka mji kwa makali ya upanga, lakini wakamuacha mtu huyo na ndugu zake
wote waondoke. 26 Na mtu huyo akaenda nchi ya Wahiti, akajenga mji, akauita Luzu,
ambalo jina lake hata leo. 27 Watu wa Manase hawakuwafukuza watu waliokuwa
katika miji ya Bethsheani na vijiji vyake, au Taanaki na vijiji vyake, au wale waliokaa

Dori na vijiji vyake, wala wale waliokaa Ibleamu na vijiji vyake, wala walioshi Megido
na vijiji vyake, kwa sababu Wakanaani walikuwa wameamua kuishi katika nchi
hiyo. 28 Israeli ipokuwa na nguvu, waliwalazimisha Wakanaani wawatumikie kwa
kazi ngumu, lakini hawakuwafukuza kabisa. 29 Efraimu hakuwafukuza Wakanaani
waliokaa Gezeri; kwa hiyo Wakanaani wakakaa kati yao. 30 Zebuloni hakuwafukuza
watu wa Kitroni, wala watu waliokuwa Nahaloli; na Wakanaani wakaendelea kuishi
pamoja nao; lakini Zabuloni akawalazimisha Wakanaani wawatumikie kwa kazi
ngumu. 31 Asheri hakuwafukuza watu wanaoishi Aka, au watu wanaoishi Sidoni, au
wale wanaoishi Alabu, Akzib, Helba, Afeka, au Rehobu. 32 Kwa hiyo kabila ya Asheri
iliishi kati ya Wakanaani (waliokaa katika nchi hiyo), kwa sababu hawakuwafukuza.
33 Na kabila la Naftali halikuwafukuza watu waliokuwa wakiishi Bethshemeshi, wala
waliokuwa wakiishi Bethanathi. Kwa hiyo kabila la Naftali liliishi kati ya Wakanaani
(watu waliokuwa wakiishi katika nchi hiyo). Hata hivyo, wenyeji wa Bethshemeshi
na Bethanathi walilazimishwa kufanya kazi ngumu kwa Naphthali. 34 Waamori
waliwalazimisha kabila la Dani kuishi katika nchi ya kilima, hawakuwaruhusu
kuja bondeni. 35 Basi Waamori waliishi katika mlima wa Heresi, huko Aiyaloni,
na Shaalbimu, lakini nguvu za kijeshi za nyumba ya Yusufu ziliwashinda, nao
wakalazimishwa kuwatumikia kwa kazi ngumu. 36 Mpaka wa Waamori ulikuwa
kutoka kilima cha Akrabimu huko Sela hadi nchi ya vilima.

# 2

1 Malaika wa Bwana akatoka Gilgali, akaenda Bokimu, akasema, “Nimekuleta
kutoka Misri, na nimekuleta katika nchi niliyoapa kuwapa baba zako. 2 Nikasema,
'Sitakuvunja kamwe agano langu na wewe. Usifanye agano na wale wanaoishi
katika nchi hii. Ziangushe madhabahu zao. Lakini hukusikiliza sauti yangu. Je!
ni nini hiki ulichokifanya? 3 Basi sasa nasema, “Sitawafukuza Wakanaani mbele
yenu, nao watakuwa miiba kwenu, na miungu yao itakuwa mtego kwa ajili yenu.”
4 Malaika wa Bwana alipowaambia maneno hayo kwa watu wote wa Israeli, watu
wakapiga kelele na kulia. 5 Waliita mahali hapo Bokimu. Hapo wakatoa dhabihu
kwa Bwana. 6 Yoshua alipowaruhusu watu waende zao, wana wa Israeli kila
mmoja akaenda mahali alipopewa, wakiwa na umiliki wa ardhi yao. 7 Watu
walimtumikia Bwana wakati wa maisha ya Yoshua na wazee walioendelea baada
yake, ni wale waliokuwa wameona matendo yote makuu ya Bwana aliyoyafanya
kwa Israeli. 8 Yoshua mwana wa Nuni, mtumishi wa Bwana, alikufa akiwa na umri
wa miaka 110. 9 Wakamzika ndani ya mpaka wa nchi aliyopewa huko Timnath
Heresi, katika mlima wa Efraimu, kaskazini mwa Mlima Gaash. 10 Kizazi hicho
chote kilikusanyika kwa baba zao. Kizazi kingine kilichofuata baada yao ambao
hakikumjua Bwana au kile alichokifanya kwa Israeli. 11 Watu wa Israeli walifanya
yaliyo mabaya machoni pa Bwana, nao wakawatumikia Mabaali. 12 Wakaondoka
kwa Bwana, Mungu wa baba zao, aliyewatoa kutoka Misri. Wakaifuata miungu
mingine, miungu ya watu waliokuwa karibu nao, nao wakaisujudia. Wakamkasirisha
BWANA kwa sababu 13 waliondoka kwa Bwana na kumwabudu Baal na Maashtoreti.
14 Hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli, naye akawapa washambuliaji walioiba
mali zao kutoka kwao. Aliwauza kama watumwa waliofanyika kwa nguvu za maadui
zao waliowazunguka, hivyo hawakuweza kujikinga dhidi ya adui zao. 15 Israeli
walipokwenda kupigana, mkono wa Bwana ulikuwa dhidi yao kuwashinda, kama
alivyowaapia. Na walikuwa katika shida kali. 16 Ndipo Bwana akawainua waamuzi,
waliowaokoa katika mikono ya wale waliokuwa wakiba mali zao. 17 Hata hivyo
hawakuwasikiliza waamuzi wao. Hawakuwa waaminifu kwa Bwana na wakajitoa
wenyewe kama makahaba kwa miungu mingine na kuabudu. Waligeuka upesi na

kuiacha njia waliyoishi baba zao-wale waliotii amri za Bwana-lakini wao wenyewe
hawakufanya hivyo. 18 Bwana aliinua waamuzi kwa ajili yao, Bwana akawasaidia
waamuzi na kuwakomboa kutoka kwa mikono ya adui zao siku zote muamuzi
aliishi. Bwana aliwahurumia walipougua kwa sababu ya wale waliowadhulumu na
kuwasumbua. 19 Lakini mwamuzi alipokufa, waligeuka na kufanya mambo ambayo
yalikuwa mabaya zaidi kuliko baba zao walivyofanya. Wakaenda kuifuata miungu
mingine kuitumikia na kuiabudu. Walikataa kuacha matendo yao yote mabaya au
njia zao za ukaidi. 20 Hasira ya Bwana iliwaka juu ya Israeli; akasema, Kwa sababu
taifa hili limevunja masharti ya agano langu ambalo nililiweka kwa ajili ya baba zao-
kwa sababu hawakuisikiliza sauti yangu. 21 Tangu sasa sitaliondoa mbele yao taifa
lolote aliloliacha Yoshua baada ya kufa. 22 Nitafanya hivi ili kuwajaribu Israeli, ikiwa
watafuata njia ya Bwana au sivyo, kama vile baba zao walivyoifuata. 23 Ndiyo sababu
Bwana aliwaacha mataifa hayo, wala hakuwafukuza haraka na kuwatia mikononi
mwa Yoshua.

# 3

1 Sasa Bwana aliyaacha mataifa haya yaijaribu Israeli, yaani kila mtu katika Israeli
ambaye hakushiriki vita yoyote huko Kanaani. 2 (Alifanya hivyo ili kuwafundisha vita
kizazi kipya cha Waisraeli ambao hawakujua kabla). 3 Haya ndio mataifa: wafalme
watano kutoka kwa Wafilisti, Wakanaani wote, Wasidoni, na Wahivi waliokaa milima
ya Lebanoni, kutoka Mlima Baali Hermoni hadi Hamathi. 4 Mataifa haya yaliachwa
kama njia ambayo Bwana angeijaribu Israeli, kuthibitisha kama watazitii amri
alizowapa babu zao kupitia Musa. 5 Basi wana wa Israeli wakakaa kati ya Wakanaani,
na Wahiti, na Waamori, na Waperizi, na Wahivi, na Wayebusi. 6 Waliwachukua binti
zao kuwa wake zao, nao wakawapa wana wao binti zao, nao wakaitumikia miungu
yao. 7 Wana wa Israeli walifanya yaliyo mabaya machoni pa Bwana, wakamsahau
Bwana, Mungu wao. Waliabudu Baali na Asherah. 8 Basi, hasira ya Bwana ikawaka
juu ya Israeli, naye akawauza mkononi mwa Kushan-rishathaimu mfalme wa Aram
Naharaimu. Watu wa Israeli walitumikia Kushan Rishathaimu kwa miaka nane.
9 Watu wa Israeli walipomwomba Bwana, Bwana akamuinua mtu atakayewasaidia
wana wa Israeli, na mtu atakayewaokoa: Othnieli mwana wa Kenazi (ndugu mdogo
wa Kalebu). 10 Roho wa Bwana akamtia nguvu, naye akahukumu Israeli na akatoka
kwenda vitani. Bwana akampa kuishinda Kush-rishataimu mfalme wa Aramu.
Mkono wa Othnieli alishinda Kushan Rishathaimu. 11 Nchi ilikuwa na amani kwa
miaka arobaini. Ndipo Otinieli mwana wa Kenazi akafa. 12 Baada ya hayo, Waisraeli
wakafanya yaliyo mabaya machoni pa Bwana; Bwana akampa Egloni mfalme wa
Moabu nguvu, kuwashinda Waisraeli. 13 Eglon alijiunga na wana wa Amoni na
Waamaleki wakaenda na kuwashinda Israeli, na walichukua mji wa Mitende. 14 Watu
wa Israeli walimtumikia Eglon mfalme wa Moabu kwa miaka kumi na nane. 15 Wana
wa Israeli walipomwomba Bwana, Bwana akamwinua mtu aliyewasaidia, Ehudi
mwana wa Gera, Mbenjamini, mtu shoto. Wana wa Israeli wakamtuma kwa Egloni,
mfalme wa Moabu, kwa malipo yao ya kodi. 16 Ehudi akajifanyia upanga uliokuwa
na makali kuwili, urefu wa dhiraa moja; aliufunga chini ya nguo zake juu ya mguu
wake wa kulia. 17 Akampa Egloni Mfalme wa Moabu malipo ya kodi. (Egloni
alikuwa mtu mnene sana.) 18 Baada ya Ehudi kulipa malipo ya kodi, aliondoka
na wale waliokuwa wameibeba. 19 Hata hivyo Ehudi mwenyewe, alipofikia mahali
ambapo sanamu za kuchonga zilitengenezwa karibu na Gilgali, akageuka na kurudi,
akasema, 'Nina ujumbe wa siri kwako, mfalme wangu.' Eglon akasema, 'Nyamazeni
kimya!' Kwa hiyo wote waliomtumikia wakatoka kwenye chumba. 20 Ehudi akaja
kwake. Mfalme alikuwa amekaa peke yake, peke yake katika chumba cha juu cha
baridi. Ehudi akasema, 'Nina ujumbe kutoka kwa Mungu kwa ajili yeko.' Mfalme

akasimama kutoka katika kiti chake. [21] Ehudi akanyoosha mkono wake wa kushoto
na akachukua upanga kutoka mguu wake wa kulia, na akautia ndani ya mwili
wa mfalme. [22] Na kipini cha upanga kikaingia ndani yake baada ya upanga, nao
ukatokea nyuma yake, na mafuta yakashikamana juu ya upanga, kwa kuwa Ehudi
hakuutoa upanga nje ya mwili wake. [23] Kisha Ehudi akatoka kwenye ukumbi na
akafunga milango ya chumba cha juu nyuma yake na akawafungia. [24] Baada ya
Ehudi kuondoka, watumishi wa mfalme wakaja; wakaona milango ya chumba cha
juu imefungwa, kwa hiyo wakafikiri, 'Hakika atakuwa anajitoa mwenyewe katika hali
ya baridi ya chumba cha juu.' [25] Walizidi kuwa na wasiwasi hata walipoanza kuhisi
kuwa walikuwa wakipuuza wajibu wao wakati mfalme bado hakufungua milango
ya chumba cha juu. Kwa hiyo walichukua ufunguo wakawafungua, tazama bwana
wao, ameanguka chini, amekufa. [26] Wakati watumishi wakisubiri, wakijiuliza nini
wanapaswa kufanya, Ehudi alikimbia na kupita mahali ambako kulikuwa na sanamu
za kuchonga, na hivyo akakimbia kwenda Seira. [27] Alipofika, alipiga tarumbeta
katika nchi ya mlima wa Efraimu. Kisha wana wa Israeli wakashuka pamoja naye
kutoka milimani, naye akawaongoza. [28] Akawaambia, Nifuate, kwa kuwa Bwana
atawashinda adui zenu, Wamoabu. Wakamfuata, wakakamata vivuko vya Bonde la
Yordani, toka kwa Wamoabi, wala hawakuruhusu mtu yeyote kuvuka mto. [29] Wakati
huo waliwaua watu elfu kumi wa Moabu, na wote walikuwa watu wenye nguvu
na wenye uwezo. Hakuna aliyekimbia. [30] Kwa hiyo siku hiyo Moabu ilishindwa na
nguvu ya Israeli. Na nchi ilikuwa na amani kwa miaka thelathini. [31] Baada ya Ehudi,
mwamuzi aliyefuata alikuwa Shamgari mwana wa Anathi ambaye aliwaua Wafilisti
600 kwa konzo la ng'ombe. Pia aliwaokoa Israeli kutoka kwenye hatari.

# 4

[1] Baada ya Ehudi kufa, watu wa Israeli walifanya tena yaliyo mabaya machoni pa
Bwana. [2] Bwana akawatia mkononi mwa Yabini, mfalme wa Kanaani, aliyewala huko
Hasori. Kamanda wa jeshi lake aitwaye Sisera, naye aliishi Harosheti ya Mataifa.
[3] Wana wa Israeli wakamwomba Bwana awasaidie, kwa sababu Sisera alikuwa
na magari ya chuma mia tisa na akawashinda wana wa Israeli kwa nguvu kwa
miaka ishirini. [4] Basi Debora, nabii wa kike (mke wa Lapidothi), alikuwa mwamuzi
anayeongoza katika Israeli wakati huo. [5] Naye aliketi chini ya mtende wa Debora
kati ya Rama na Betheli katika nchi ya mlima wa Efraimu, na watu wa Israeli
walimwendea ili kutatua migogoro yao. [6] Akamtuma Baraka mwana wa Abinoamu
kutoka Kedeshi huko Naftali. Akamwambia, Bwana, Mungu wa Israeli, anakuamuru,
Nenda katika mlima wa Tabori, uende pamoja nawe watu elfu kumi kutoka Naftali
na Zabuloni. [7] Nitamfukuza Sisera, jemadari wa jeshi la Yabini, akutane nawe karibu
na mto Kishoni, pamoja na magari yake na jeshi lake, na nitakupa ushindi juu
yake. ' [8] Baraka akamwambia, 'Ikiwa utakwenda nami, nitakwenda, lakini ikiwa
huendi pamoja nami, sitaenda.' [9] Alisema, 'Nitakwenda nawe. Hata hivyo, njia
unayoienda haitakupa heshima wewe, kwa kuwa Bwana atamuuza Sisera mkononi
mwa mwanamke. Ndipo Debora akainuka, akaenda pamoja na Baraka Kedeshi.
[10] Baraki akawaita wana wa Zebuloni na Naftali kusanyika Kedeshi. Watu elfu kumi
walimfuata, na Debora akaenda pamoja naye. [11] Heberi (Mkeni) alijitenganisha
na Wakeni - walikuwa wazao wa Hobabu (mkwe wa Musa) - na akaweka hema
yake mwaloni uliopo huko Saanaimu karibu na Kedesh. [12] Walipomwambia Sisera
kwamba Baraka, mwana wa Abinoamu, alikuwa amekwenda mlima wa Tabori,
[13] Sisera akawaita magari yake yote, magari ya farasi mia tisa, na askari wote
waliokuwa pamoja naye, kutoka Haroshethi ya Mataifa mpaka Mto Kishoni. [14] Debora
akamwambia Baraka, Nenda! Kwa maana hii ndiyo siku ambayo Bwana amekupa

ushindi juu ya Sisera. Je! si Bwana anayekuongoza? Basi Baraka akashuka
kutoka mlima wa Tabori na watu kumi elfu wakamfuata. 15 Bwana alifanya jeshi
la Sisera kuchanganyikiwa, magari yake yote, na jeshi lake lote. Watu wa Baraka
waliwashinda na Sisera akaanguka kutoka kwenye gari lake na kukimbia kwa miguu.
16 Lakini Baraka akayafuata magari na jeshi mpaka Haroshethi ya Mataifa, na jeshi
lote la Sisera likauawa kwa upanga, wala hakuna mtu aliyeokoka. 17 Lakini Sisera
akakimbia kwa miguu mpaka hema ya Yaeli, mkewe Heberi Mkeni; kwa sababu
kulikuwa na amani kati ya Yabini mfalme wa Hazori, na nyumba ya Heberi Mkeni.
18 Jaeli akatoka kumlaki Sisera, akamwambia, karibu, bwana wangu; karibu kwangu,
wala usiogope. Basi akakaribia kwake, akaingia hemani kwake, naye akamvika
bushuti. 19 Akamwambia, Tafadhali nipe maji kidogo ninywe, kwa maana nina
kiu. Alifungua mfuko wa ngozi ya maziwa akampa anywe, kisha akamfunika tena.
20 Akamwambia, “Simama mlangoni pa hema. Ikiwa mtu atakuja na kukuuliza,
'Je, kuna mtu hapa?', Sema 'Hapana'.” 21 Kisha Jaeli (mke wa Heberi) akachukua
kigingi cha hema na nyundo mkononi mwake akamwendea kwa siri, kwa sababu
alikuwa amelala usingizi mzito, naye akakitia kigingi cha hema upande wa kichwa
chake akamchoma na kikapenya kushuka chini. Hivyo akafa. 22 Baraka alipokuwa
akimfuata Sisera, Jaeli alitoka kukutana naye akamwambia, “Njoo, nitakuonyesha
mtu unayemtafuta.” Basi akaingia pamoja naye, tazama Sisera amekufa, na kigingi
cha hema kando ya kichwa chake. 23 Basi siku hiyo Mungu alimshinda Jabin, mfalme
wa Kanaani, mbele ya watu wa Israeli. 24 Uwezo wa watu wa Israeli ulikua na nguvu
zaidi dhidi ya Jabin mfalme wa Kanaani, hata walipomwangamiza.

# 5

1 Siku hiyo Debora na Baraka, mwana wa Abinoamu waliimba wimbo huu:
2 'Viongozi wanapoongoza mbele ya Israeli, watu wanapojitolea kupigana vita,
tunamsifu Bwana! 3 Sikiliza, ninyi wafalme! Sikiliza kwa makini, ninyi viongozi!
Mimi nitamwimbia Bwana; Nami nitamsifu Bwana, Mungu wa Israeli. 4 Ee Bwana,
wakati ulipotoka Seiri, ulipokwenda kutoka Edomu, nchi ilitetemeka, na mbingu
pia ilitetemeka; pia mawingu yalitoa maji. 5 Milima ikatoka mbele ya uso wa
Bwana; hata Mlima Sinai ukatetemeka mbele ya uso wa Bwana, Mungu wa Israeli.
6 Katika siku za Shamgari (mwana wa Anathi), katika siku za Jael, barabara kuu
ziliachwa, na wale ambao walitembea tu walitumia njia za upepo. 7 Kulikuwa na
mashujaa wachache huko Israeli, mpaka mimi, Debora, nilipochukua amri- mama
alichukua amri katika Israeli! 8 Walichagua miungu mpya, kulikuwa na vita katika
malango ya jiji lakini bado hapakuwa na ngao au mikuki iliyoonekana kati ya
watu elfu arobaini nchini Israeli. 9 Moyo wangu unawaendea wakuu wa Israeli,
pamoja na watu ambao walijitolea -tunambariki Bwana kwa ajili yao! 10 Fikiria
juu ya hili- ninyi ambao hupanda punda weupe mmeketi kwenye mazulia, nanyi
mnaotembea njiani. 11 Sikiliza sauti za wale wanaoimba kwenye maeneo ya kutekea
maji. Huko wanasema tena juu ya matendo ya haki ya Bwana, na matendo ya haki ya
wapiganaji wake katika Israeli. Ndipo watu wa Bwana wakashuka kwenye malango
ya mji. 12 Amka, amka, Debora! Amka, amka, imba wimbo! Simama, Baraka,
na uwakamate wafungwa wako, wewe mwana wa Abinoamu. 13 Wale waliokoka
wakaja chini kwa watu wenye nguvu; watu wa Bwana walikuja kwangu pamoja
na mashujaa. 14 Walikuja kutoka Efraimu, ambao mizizi yao iko katika Amaleki;
watu wa Benyamini walikufuata. Wakuu wa Makiri walitoka, na kutoka Zebuloni
wale wanaobeba fimbo ya afisa. 15 Na wakuu wangu katika Isakari walikuwa
pamoja na Debora; na Isakari alikuwa na Baraka waliingia bobdeni kwa kasi chini
ya amri yake. Miongoni mwa jamaa za Reubeni kulikuwa na utafutaji mkubwa

wa moyo. 16 Kwa nini uliketi katikati ya moto, ukisikiliza wachungaji wakipiga
filimbi yao kwa makundi yao? Na kwa jamaa za Reubeni kulikuwa na utafutaji
mkubwa wa moyo. 17 Gileadi alikaa upande wa pili wa Yordani; na Dani, kwa
nini alizunguka juu ya meli? Asheri alibakia pwani na akaishi karibu na bandari
zake. 18 Zabuloni lilikuwa kabila ambayo lingeweza kuhatarisha maisha yao mpaka
kufikia kifo, Nafthali, pia, katika uwanja wa vita. 19 Wafalme walikuja, wakapigana;
wafalme wa Kanaani wakapigana huko Taanaki karibu na maji ya Megido. Lakini
hawakuondoa fedha kama nyara. 20 Nyota zilipigana kutoka mbinguni, kutoka katika
njia zao za mbinguni zilipigana na Sisera 21 Mto Kishoni uliwaondoa, mto ule wa
kale, Mto Kishoni. Endelea mbele nafsi yangu, jipe nguvu! 22 Kisha sauti za hofu
za farasi-kupiga mbio, kupigana kwa watu wake wenye nguvu. 23 'Ilaani Meroz!'
asema malaika wa Bwana. 'Hakika walaani wenyeji wake!' Kwa sababu hawakuja
kumsaidia Bwana, kumsaidia Bwana katika vita dhidi ya mashujaa wenye nguvu.
24 Yaeli amebarikiawa zaidi kuliko wanawake wengine wote, Yaeli (mke wa Heberi
Mkeni), amebarikiwa zaidi kuliko wanawake wote wanaoishi katika hema. 25 Mtu
yule aliomba maji, naye akampa maziwa; akamletea siagi katika sahani inayofaa
kwa wakuu. 26 Aliweka mkono wake kwenye kigingi cha hema, na mkono wake wa
kuia katika nyundo ya mfanyakazi; kwa nyundo akampiga Sisera, alimpiga kichwani
kwake. Aliligawanya fuvu lake vipande vipande wakati alipompiga pembeni ya
kichwa chake. 27 Akaanguka katikati ya miguu yake, akaanguka akalala pale. Kati ya
miguu yake akaanguka. Mahali alipoanguka ni pale ambapo aliuawa kwa ukatili.
28 Aliangalia dirishani - mama yake Sisera aliangalia kupitia kamba na akasema
kwa huzuni, 'Kwa nini gari lakelimechelewa kuja? Kwa nini viboko vya farasi
vinavyovuta magari yake vimechelewa? ' 29 Wafalme wake wenye hekima walijibu,
na yeye mwenyewe akajibu jibu lile 30 'Je, hawakupata na kugawanya nyara? Tumbo,
matumbo mawili kwa kila mtu; nyara ya kitambaa kilichofunikwa kwa Sisera, nyara
ya kitambaa kilichofunikwa, nguo mbili za rangi iliyofunikwa kwa misumari ya wale
waliopora? 31 Naam, adui zako wote wataangamia, Ee Bwana! Lakini marafiki zako
watakuwa kama jua wakati linapoongezeka kwa uwezo wake. Na nchi ikawa na
amani kwa miaka arobaini.

# 6

1 Wana wa Israeli wakafanya yaliyo mabaya machoni pa Bwana; naye akawatia
mikononi mwa Midiani kwa miaka saba. 2 Uwezo wa Midiani uliwanyanyasa Israeli.
Kwa sababu ya Midiani, watu wa Israeli walitengeneza makao wenyewe kutoka
kwenye mabwawa katika milima, mapango, na ngome. 3 Kisha ikawa kwamba
wakati wowote Waisraeli walipopanda mazao yao, Wamidiani na Waamaleki na
watu kutoka mashariki waliwavamia Waisraeli. 4 Waliweza kutengenezajeshi lao
juu ya ardhi na kuharibu mazao, mpaka njia ya Gaza. Hawakuacha chakula huko
Israeli, wala kondoo wala ng'ombe wala punda. 5 Kila wakati wao na mifugo yao na
mahema walipokuja, walikuja kama kundi la nzige, na haikuwezekana kuhesabu
watu au ngamia zao. Walivamia ardhi ili kuiharibu. 6 Midiani iliwadhoofisha
Waisraeli sana mpaka watu wa Israeli wakamwita Bwana. 7 Watu wa Israeli
walipomwomba Bwana kwa sababu ya Midiani, 8 Bwana alimtuma nabii kwa wana
wa Israeli. Nabii akawaambia, Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, Nimekuleta
kutoka Misri; Nilikutoa nje ya nyumba ya utumwa. 9 Naliwaokoa kutoka kwenye
mikono ya Wamisri, na kutoka kwenye mkono wa wote waliokuwa wakikunyanyasa.
Niliwafukuza mbele yenu, na nimewapa nchi yao. 10 Niliwaambia, “Mimi ndimi
Bwana, Mungu wenu; Nimewaamuru msiabudu miungu ya Waamori, ambao mnaishi
katika nchi yao. Lakini hamkuitii sauti yangu.” 11 Basi malaika wa Bwana akaja

na kukaa chini ya mwaloni huko Ofra, uliokuwa wa Yoashi (Mwabiyezeri), wakati
Gidioni, mwana wa Yoashi, akitenganisha ngano katika sakafu, katika kikapu cha
divai-kuificha toka kwa Wamidiani. 12 Malaika wa Bwana akamtokea, akamwambia,
Bwana yu pamoja nanyi, mpiganaji mwenye nguvu! 13 Gideoni akamwambia, Oo,
bwana wangu, ikiwa Bwana yu pamoja nasi, kwa nini basi yote haya yanatupata? Je,
yako wapi matendo yake yote mazuri ambayo baba zetu walituambia, waliposema,
'Je! si Bwana aliyetukomboa kutoka Misri?' Lakini sasa Bwana ametuacha na
kututia mikononi mwa Midiani. ' 14 Bwana akamtazama na kusema, “Nenda
katika nguvu uliyo nayo tayari. Uiokoe Israeli kutoka mkononi wa Midiani. Je,
sikukutuma?” 15 Gideoni akamwambia, “Tafadhali, Bwana, nawezeje kuwaokoa
Israeli? Angalia, familia yangu ni dhaifu zaidi katika Manase, na mimi si muhimu
katika nyumba ya baba yangu.” 16 Bwana akamwambia, “Nitakuwa pamoja nawe,
nawe utalishinda jeshi lote la Midiani kama mtu mmoja.” 17 Gideoni akamwambia,
“Ikiwa unapendezwa na mimi, nipe basi ishara kwamba wewe ndio unenena
nami. 18 Tafadhali, usiondoke hapa, mpaka nitakapokuja kwako na kuleta zawadi
yangu na kuiweka mbele yako.” Bwana akasema, “Nitasubiri mpaka utakaporudi.”
19 Gideoni akaenda, akaandaa mwana mbuzi, na efa moja ya unga akafanya mikate
isiyotiwa chachu. Akaiweka nyama hiyo katika kikapu, na akaweka mchuzi ndani
ya sufuria na kuviletea chini ya mti wa mwaloni, akavitowa. 20 Malaika wa Mungu
akamwambia, “Chukua nyama na mikate isiyotiwa chachu, ukaweke juu ya mwamba
huu, ukamwage mchuzi juu yake.” Gideoni akafanya hivyo. 21 Kisha malaika wa
Bwana akashika ncha ya fimbo mkononi mwake. Kwa hiyo akagusa nyama na
mikate isiyotiwa chachu; moto ukatoka nje ya mwamba, ukateketeza nyama na
mikate isiyotiwa chachu. Kisha malaika wa Bwana akaenda, na Gideoni hakuweza
kumwona tena. 22 Gideoni alielewa kuwa yule alikuwa malaika wa Bwana. Gideoni
akasema, “Ewe Bwana MUNGU! Kwa maana nimemwona malaika wa Bwana uso
kwa uso!” 23 Bwana akamwambia, “Amani iwe kwako! Usiogope, huwezi kufa.”
24 Basi Gideoni akamjengea Bwana madhabahu huko. Aliiita, “Bwana ni Amani.”
Hadi leo bado iko katika Ofra ya jamaa ya Waabiezeri. 25 Usiku huo, Bwana
akamwambia, “Twaa ng'ombe wa baba yako, na ng'ombe wa pili wa umri wa
miaka saba, ukaondoe madhabahu ya Baali, ambayo ni ya baba yako, na kukata
Ashera iliyo karibu nayo. 26 Jenga madhabahu kwa Bwana, Mungu wako juu ya
mahali pa kukimbilia, na kuijenga njia sahihi. Toa ng'ombe ya pili kama sadaka
ya kuteketezwa, ukitumia kuni kutoka Ashera uliyoikata. ' 27 Gideoni akachukua
watumishi wake kumi na kufanya kama Bwana alivyomwambia. Lakini kwa sababu
aliogopa sana watu wa nyumba ya baba yake na watu wa mji hakufanya hivyo
wakati wa mchana, alifanya hivyo usiku. 28 Asubuhi wakati watu wa mji walipoamka,
madhabahu ya Baali imebomolewa, na Ashera iliyokuwa karibu nayo imekatwa, na
ng'ombe wa pili ametolewa sadaka kwenye madhabahu iliyojengwa. 29 Watu wa mji
wakaambiana, “Ni nani aliyefanya jambo hili?” Walipokuwa wakiongea na wengine
na kutafuta majibu, wakasema, 'Gidioni mwana wa Yoashi amefanya jambo hili.”
30 Ndipo watu wa mji wakamwambia Yoashi, “Mtoe mtoto wako ili afe, kwa sababu
ameibomoa madhabahu ya Baali, na kwa sababu ameikata Ashera karibu nayo.”
31 Yoashi akawaambia wote waliompinga, “Je, ninyi mtamsihi Baali? Je, mtamuokoa?
Mtu yeyote atakayemtetea, basi atauawa asubuhi hii. Ikiwa Baali ni mungu, basi
atajitetea mwenyewe wakati mtu anaibomoa madhabahu yake.” 32 Kwa hiyo siku
hiyo wakamwita Gideoni “Yerubaali,” kwa sababu alisema, “Baali ajiijitetee dhidi
yake,” kwa sababu Gidioni alivunja madhabahu ya Baali. 33 Basi Wamidiani wote,
Waamaleki, na watu wa mashariki walikusanyika pamoja. Wakavuka Yordani na
wakapanga katika bonde la Yezreeli. 34 Lakini Roho wa Bwana akaja juu ya Gideoni.

Gideoni akapiga tarumbeta, akawaita jamaa ya Abiezeri, ili wapate kumfuata.
[35] Aliwatuma wajumbe wote katika Manase, na wao pia, waliitwa nje kumfuata.
Naye akatuma wajumbe kwa Asheri, na Zabuloni, na Naftali; nao wakaenda kumlaki.
[36] Gideoni akamwambia Mungu, “Ikiwa ungependa kunitumia kuokoa Israeli, kama
ulivyosema, [37] tazameni, ninaweka ngozi ya samazi kwenye sakafu. Ikiwa kuna
umande tu juu ya ngozi, na ni kavu duniani, basi nitajua kwamba utanitumia kuokoa
Israeli, kama ulivyosema.” [38] Hivi ndivyo ilivyotokea-Gideoni aliamka mapama
asubuhi, akaikamua ngozi hiyo, na akatoa umande kwenye ngozi, wa kutosha kujaza
bakuli kwa maji. [39] Gideoni akamwambia Mungu, 'Usinikasirikie, nitasema tena kwa
mara nyingine. Tafadhali niruhusu nijaribu tena kwa kutumia ngozi. Wakati huu
uifanye kavu, na iwe na umande juu ya ardhi yote kuzunguka. [40] Mungu alifanya
kile alichoomba usiku huo. Ngozi ilikuwa kavu, na kulikuwa na umande katika ardhi
yote iliyozunguka.

# 7

[1] Ndipo Yerubaali (yaani Gideoni) akainuka mapema, na watu wote waliokuwa
pamoja naye, wakaweka kambi kando ya chemchemi ya Harodi. Kambi ya Midiani
ilikuwa kaskazini mwao katika bonde karibu na kilima cha More. [2] Bwana
akamwambia Gideoni, Kuna askari wengi sana kwa mimi kukupa ushindi juu ya
Wamidiani, ili Waisraeli wasijisifu juu yangu, wakisema, 'Nguvu zetu zimetuokoa'.
[3] Basi, tangaza masikioni mwa watu, ukisema, Yeyote anayeogopa, anayetetemeka,
arudi na atoke katika mlima Gileadi. 'Basi, watu elfu ishirini na mbili wakaondoka,
na elfu kumi wakabaki. [4] Bwana akamwambia Gideoni, 'Watu bado ni wengi sana.
Wapeleke chini kwenye maji, na nitafanya idadi yao iwe ndogo kwa ajili yako. Kama
nikisema, 'Huyu atakwenda pamoja nawe,' atakwenda pamoja nawe; lakini kama
nikisema, 'Huyu hawezi kwenda pamoja nawe,' hatakwenda. ' [5] Gideoni akawapeleka
watu kwenye maji; Bwana akamwambia, “Ondoa kila mtu atakayelamba maji, kama
mbwa alambavyo, kutoka kwa wale wanaopiga magoti na kunywa.” [6] Wanaume mia
tatu walilamba. Wengine wote walipiga magoti kunywa maji. [7] Bwana akamwambia
Gideoni, “Kwa watu hawa mia tatu waliokwisha kulamba maji, nitakuokoa na kukupa
ushindi juu ya Wamidiani. Acha kila mtu arudi mahali pake.” [8] Kwa hiyo wale
waliochaguliwa walichukua vifaa vyao na tarumbeta zao. Gideoni akawarudisha
watu wote wa Israeli, kila mtu kwenda kwenye hema yake, lakini akawaweka watu
mia tatu. Basi kambi ya Midiani ilikuwa chini yake katika bonde. [9] Usiku huo
huo Bwana akamwambia, “Simama! Kavamie kambi, kwa maana nitakupa ushindi
juu yake. [10] Lakini ikiwa unaogopa kushuka, shka kwenye kambi pamoja na Purh
mtumishi wako, [11] na usikilize kile wanachosema, na ujasiri wako utaimarishwa
kushambulia kambi.” Basi Gidioni akaenda pamoja na Pura mtumishi wake, mpaka
chini kwa walinzi wa kambi. [12] Wamidiani, Waamaleki, na watu wote wa mashariki
walikaa karibu na bonde, wengi kama wingu la nzige. Ngamia zao walikuwa zaidi
ya mawingu; walikuwa zaidi kuliko idadi ya mchanga katika bahari. [13] Gideoni
alipofika huko, mtu alikuwa akimwambia mwenzake ndoto. Mtu huyo akasema,
“Angalia! Niliota ndoto, na nikaona mkate wa shayiri umeanguka ndani ya kambi ya
Midiani. Ukaja hemani, na kuipiga kwa nguvu sana hata ikaanguka chini ikapinduka
na kulala chini. ' [14] Mtu mwingine akasema, 'Hii si kitu kingine isipokuwa upanga
wa Gideoni (mwana wa Yoashi), Mwisraeli. Mungu amempa ushindi juu ya Midiani
na jeshi lake lote. ' [15] Gideoni aliposikia habari ya ile ndoto na tafsiri yake, akainama
chini na kuabudu. Alirudi kwenye kambi ya Israeli na kusema, “Simameni! Bwana
ametupa ushindi juu ya jeshi la Midiani.” [16] Akawagawa watu mia tatu katika
makundi matatu, na akawapa tarumbeta zote na mitungi tupu, na taa ndani ya

kila mtungi. 17 Akawaambia, 'Niangalieni mimi na kufanya yale ninayoyafanya.
Tazama! Ninapofika kwenye mwisho wa kambi, ni lazima mfanye kile ninachofanya.
18 Nitakapopiga tarumbeta, mimi na wote Mlio pamoja nami, basi mtapiga tarumbeta
zenu katika kila upande wa kambi nzima na kupiga kelele, “Kwa Bwana na Gideoni!”
19 Basi Gideoni na watu mia moja waliokuwa pamoja naye walifika mwisho wa
kambi, hapo mwanzoni mwa saa ya kati. Wakati Wamidiani walikuwa wakibadilisha
walinzi, walipiga tarumbeta na kuvunja mitungi iliyokuwa mikononi mwao. 20 Vikosi
vitatu vilipiga tarumbeta na kuvunja mitungi. Walikuwa na taa katika mikono yao
ya kushoto na tarumbeta katika mikono yao ya kulia ili kuwapiga. Walipiga kelele,
“Upanga wa Bwana na wa Gideoni.” 21 Kila mtu alisimama mahali pake kando ya
kambi na jeshi la Midiani likakimbia. Walipiga kelele na kukimbia 22 Walipopiga
tarumbeta mia tatu, Bwana akaweka upanga wa kila mtu wa Midiani dhidi ya
wenzake na dhidi ya jeshi lake lote. Jeshi likimbia mpaka Bethshita kuelekea Serera,
mpaka mpaka wa Abel Mehola, karibu na Tabathi. 23 Watu wa Israeli kutoka Naftali,
Asheri, na Manase wote waliitwa nje, nao wakawafuata Midiani. 24 Gideoni akatuma
wajumbe katika nchi zote za mlima wa Efraimu, akisema, “Nenda chini dhidi
ya Midiani na umiliki Mto Yordani mpaka Bethbara, ukawazuie.” Basi wanaume
wote wa Efraimu walikusanyika pamoja na kuimiliki maji, mpaka Bethbara na Mto
Yordani. 25 Wakawatwaa wakuu wawili wa Midiani, Orebu na Zeebu. Wakamwua
Orebu kwenye mwamba wa Orebu, nao wakamwua Zeebu katika shinikizo la divai la
Zeebu. Wakawafuata Wamidiani, wakamletea Gideoni vichwa vya Orebu na Zeebu,
ng'ambo ya pili ya Yordani.

# 8

1 Watu wa Efraimu wakamwambia Gideoni, “Ni nini hiki umetutenda?
Haukuita wakati ulipokwenda kupigana na Midiani.” Wakamwambia kwa nguvu.
2 Akawaambia, “Nimefanya nini sasa kulinganisha na mlichofanya ninyi? Je! Mavuno
ya zabibu za Efraimu si bora zaidi kuliko mavuno ya zabibu ya Abiezeri? 3 Mungu
amewapa ushindi juu ya wakuu wa Midiani-Orebu na Zeeb! Mimi nimefanya nini
ukilinganisha na ninyi?” Hasira yao ikashuka chini aliposema hili. 4 Gideoni alikuja
Yordani na akavuka juu yake, yeye na watu mia tatu waliokuwa pamoja naye.
Walikuwa wamechoka, lakini bado waliendelea kufuatilia. 5 Akawaambia watu wa
Sukothi, “Tafadhali wape mikate kwa watu wanaonifuata, kwa kuwa wamechoka,
nami niwafuatilia Zeba na Salmuna, wafalme wa Midiani. 6 Na wakuu wakasema,
“Je, mikono ya Zeba na Salmuna sasa ipo mikononi mwako? Kwa nini tulipe jeshi
lako mikate?” 7 Gideoni akasema, “Bwana akitupa ushindi juu ya Zeba na Salmunna,
nitainyunyiza ngozi yenu kwa miiba ya jangwani na michongoma. 8 Akatoka huko,
akaenda Penieli, akawaambia watu maneno hayo hayo; lakini watu wa Penieli
wakamjibu kama watu wa Sukothi walivyojibu. 9 Akawaambia pia watu wa Penieli,
akasema, “Nitakapokuja kwa amani, nitauangusha mnara huu.” 10 Sasa Zeba na
Salmuna walikuwa huko Karkori pamoja na jeshi lao, karibu na watu elfu kumi na
tano, wote waliosalia nje ya jeshi lote la watu wa Mashariki, kwa kuwa walianguka
watu 120, 000 waliofundishwa kupigana na upanga. 11 Gideoni akapanda barabara
iliyochukuliwa na wakaazi wa hema, Noba na Yogbena. Akalishinda jeshi la adui,
kwa sababu hawakuwa wanatarajia shambulio. 12 Zeba na Salmuna walikimbia, na
Gideoni alipowafuata, akawatwaa wafalme wawili wa Midiani-Zeba na Salmunna-
na kulifanya jeshi lote kuwa na hofu. 13 Gideoni, mwana wa Yoashi, alirudi kutoka
kwenye vita kwenda kupitia Heresi. 14 Akamkimbilia kijana mmoja wa watu wa
Sukothi na kutafuta ushauri kutoka kwake. Kijana huyo alimwelezea viongozi
wa Sukothi na wazee wake, watu sabini na saba. 15 Gideoni akaja kwa watu

wa Sukothi, akasema, “Tazameni Zeba na Salmuna, ambao mlinidhihaki kwa ajili
yao, nikasema, 'Je! mmemshinda Zeba na Salmuna? Hatujui kwamba tunapaswa
kulipa jeshi lako mkate.” 16 Gideoni akawachukua wazee wa mji, naye akawaadhibu
watu wa Sukothi pamoja na miiba ya jangwa na michongoma. 17 Akaangusha
mnara wa Penieli na kuwaua watu wa mji huo. 18 Gideoni akamwambia Zeba
na Salmuna, “Ni watu wa aina gani mliwauawa Tabori?” Wakajibu, “Kama wewe
ulivyo, ndivyo walivyokuwa. Kila mmoja wao alionekana kama mwana wa mfalme.”
19 Gideoni akasema, 'Wao walikuwa ndugu zangu, wana wa mama yangu. Kama
Bwana anaishivyo, kama mngewaacha hai, nisingewauwa.” 20 Akamwambia Yetheri
(mzaliwa wake wa kwanza), “Simama uwaue!” Lakini kijana huyo hakutoa upanga
wake kwa kuwa aliogopa, kwa sababu alikuwa bado kijana mdogo. 21 Ndipo Zeba
na Salmuna wakasema, simama mwenyewe, utuue! Kwa maana kama mtu alivyo,
ndivyo zilivyo nguvu zake. Gideoni akasimama na kumwua Zeba na Salmuna. Pia
aliondoa mapambo yaliyokuwa juu ya shingo za ngamia zao. 22 Ndipo wana wa
Israeli wakamwambia Gideoni, “Ututawale, wewe, mtoto wako, na mjukuu wako;
kwa sababu umetuokoa mikononi mwa Midiani.” 23 Gideoni akawaambia, “Mimi
sitatawala juu yenu, wala mtoto wangu hatatawala juu yenu. Bwana atatawala juu
yenu.” 24 Gideoni akawaambia, “Nina haja yangu niitakayo kwenu kwamba kila
mmoja wenu atanipe pete kutoka kwenye nyara zake.” (Wamidiani walikuwa na
pete za dhahabu kwa sababu walikuwa Waishmaeli.) 25 Wakamjibu, “Tunafurahi
kukupa.” Wakatandika vazi na kila mtu akatupa pete kutoka kwenye nyara zake.
26 Uzito wa pete za dhahabu alizoomba zilikuwa shekeli 1, 700 za dhahabu. Nyara
hizi zilikuwa ni pamoja na mapambo ya makoja, vidani, nguo ya rangi ya zambarau
waliyovaa na wafalme wa Midiani, na zaidi ya minyororo iliyokuwa karibu na
shingo za ngamia zao. 27 Gideoni akafanya efodi kutoka katika pete na kuiweka
katika mji wake, huko Ofra, na Israeli wote wakaiandama kwa ukahaba na kuabudu.
Ilikuwa mtego kwa Gideoni na kwa wale walio nyumbani kwake. 28 Kwa hiyo
Midiani ilishindwa mbele ya watu wa Israeli na hawakuinua vichwa vyao tena. Na
nchi ikawa na amani kwa miaka arobaini siku za Gideoni. 29 Yerubaali, mwana
wa Yoashi, akaenda akakaa nyumbani kwake. 30 Gideoni alikuwa na wana sabini,
waliokuwa uzao wake, kwa kuwa alikuwa na wake wengi. 31 Mwanamke wake,
aliyekuwa Shekemu, akamzaa pia mwana, na Gideoni akampa jina lake Abimeleki.
32 Gideoni, mwana wa Yoashi, akafa katika uzee mzuri, akazikwa huko Ofra katika
kaburi la baba yake Joashi, wa jamaa ya Abiyezeri. 33 Ikawa, Gideoni alipokufa, watu
wa Israeli wakageuka tena na kujifanyia ukahaba wenyewe kwa kuabudu Mabaali.
Wamlifanya Baali Berith kuwa mungu wao. 34 Watu wa Israeli hawakukumbuka
kumtukuza Bwana, Mungu wao, aliyewaokoa kutoka kwa mikono ya adui zao kila
upande. 35 Hawakuweka ahadi zao kwa nyumba ya Yerubaali (yaani Gidioni), kwa
ajili ya mema yote aliyoyafanya katika Israeli.

# 9

1 Abimeleki, mwana wa Yerubaali, akaenda kwa jamaa za mama yake huko
Shekemu, akawaambia, na jamaa yote ya mama yake, 2 Tafadhali sema haya, ili
wakuu wote wa Shekemu wasikie, Ni kipi bora kwako Je, wana sabini wote wa
Yerubali kutawala juu yenu, au kwamba moja tu atawale juu yenu? Kumbuka
kwamba mimi ni mfupa na nyama yenu. 3 Ndugu za mama yake waliongea kwa niaba
yake kwa viongozi wa Shekemu, nao wakakubali kumfuata Abimeleki, wakasema,
Yeye ndiye ndugu yetu. 4 Wakampa vipande sabini vya fedha katika nyumba ya
Baali Berith; Abimeleki akazitumia kwa kuajiri watu wasio na sheria na wasiokuwa
wajinga, waliomfuata. 5 Abimeleki akaenda nyumbani kwa baba yake huko Ofra;

na juu ya jiwe moja akawaua ndugu zake sabini, wana wa Yerubaali. Yotamu ndiye
aliyebaki, mwana mdogo kabisa wa Yerubaali, kwa kuwa alijificha. 6 Wakuu wote
wa Shekemu na Beth Milo wakaungana, wakaenda kumfanya Abimeleki mfalme,
karibu na mwaloni karibu na nguzo iliyoko Shekemu. 7 Yotamu alipoambiwa
juu ya jambo hilo, akaenda, akasimama juu ya Mlima Gerizimu. Alipiga kelele
akawaambia, 'Sikilizeni, enyi viongozi wa Shekemu, ili Mungu awasikilize. 8 Siku
moja miti ilikwenda kumtia mafuta mfalme juu yao. Wakauambia mzeituni, tawala
juu yetu. 9 Lakini mti wa mizeituni ukawaambia, Je! Nitaacha mafuta yangu, ambayo
hutumiwa kuheshimu miungu na wanadamu, ili nipate kurudi na kuvuka juu ya
miti mingine? 10 Miti hiyo ikamwambia mtini, 'Njoo utawale juu yetu.' 11 Lakini
mtini ukawaambia, Je, nitaacha utamu wangu na matunda yangu mazuri, ili nipate
kurudi na kuvuka juu ya miti mingine? 12 Miti hiyo ikamwambia mzabibu, 'Njoo
utawale juu yetu.' 13 Mzabibu ukawaambia, Je, nitaacha divai yangu mpya, ambayo
hufurahisha miungu na wanadamu, na kurudi na kuvuka juu ya miti mingine?
14 Kisha miti yote ikawaambia mchanga, 'Njoo utawale juu yetu.' 15 Miti ya miiba
ikaiambia miti, 'Ikiwa unataka kunipaka mafuta niwe mfalme juu yako, njoo na
upate usalama chini ya kivuli changu. Ikiwa sivyo, basi moto lazima uondoke
kwenye mchanga na uiteketeze mierezi ya Lebanoni. ' 16 Basi, ikiwa umefanya
kweli na uaminifu, ulimfanya Abimeleki mfalme, na ikiwa umefanya vizuri juu
ya Yerubaali na nyumba yake, na ikiwa umemuadhibu kama anavyostahili, 17 - na
kufikiri kwamba baba yangu alipigana kwa ajili yenu, akahatarisha maisha yake,
na akawaokoa kutoka kwenye mkono wa Midiani - 18 lakini leo umeamka juu ya
nyumba ya baba yangu na kuwaua watoto wake, watu sabini, juu ya jiwe moja.
Na umemfanya Abimeleki, mwana wa mtumishi wake, awe mfalme juu ya wakuu
wa Shekemu, kwa sababu yeye ni ndugu yenu. 19 Ikiwa mlifanya kwa uaminifu
na uelekevu pamoja na Jerubalai na nyumba yake, basi mnapaswa kufurahi katika
Abimeleki, naye apate kufurahi ndani yenu. 20 Lakini ikiwa sio, moto utoke kwa
Abimeleki, ukawaangamize watu wa Shekemu na Beth Milo. Basi moto utoke kwa
watu wa Shekemu na Beth Milo, ili kumteketeza Abimeleki. 21 Yothamu akakimbia,
naye akaenda Beeri. Aliishi huko kwa sababu ilikuwa mbali na Abimeleki, kaka
yake. 22 Abimeleki akatawala juu ya Israeli kwa miaka mitatu. 23 Mungu alituma
roho mbaya kati ya Abimeleki na viongozi wa Shekemu. Viongozi wa Shekemu
walisaliti uaminifu waliokuwa nao kwa Abimeleki. 24 Mungu alifanya hivyo ili uhalifu
uliofanywa kwa wana sabini wa Yerubaali uweze kulipizwa kisasi, na Abimeleki
ndugu yao atawajibishwa kwa kuwaua, na watu wa Shekemu watawajibishwa kwa
sababu walimsaidia kuua ndugu zake. 25 Basi wakuu wa Shekemu wakawaweka
wanaume wamkisubiri juu ya vilima ili wamwangamize, nao wakawaibia wote
waliokuwa wamepita katika barabara hiyo. Hii iliripotiwa kwa Abimeleki. 26 Gaali
mwana wa Ebedi akenda pamoja na ndugu zake, wakavuka Shekemu. Viongozi
wa Shekemu walimwamini. 27 Wakaenda shambani wakakusanya zabibu kutoka
kwa mizabibu, nao wakazikanyaga. Walifanya sherehe katika nyumba ya mungu
wao, walikula na kunywa, kumlaani Abimeleki. 28 Gaali mwana wa Ebedi, akasema,
Abimeleki ni nani, na Shekemu ni nani, hata tumtumikie? Je, si mwana wa
Yerubaali? Na Zebuli si afisa wake? Watumikieni watu wa Hamori, baba yake
Shekemu! Kwa nini tunapaswa kumtumikia? 29 Laiti watu hawa wangekukuwa
chini ya amri yangu! Kisha ningemuondoa Abimeleki. Ningemwambia Abimeleki,
'liondoe nje jeshi lako lote.' 30 Zebul, mkuu wa mji, aliposikia maneno ya Gaali,
mwana wa Ebedi, hasira yake ikawaka. 31 Akatuma wajumbe kwa Abimeleki ili
wapate kudanganya, akisema, Tazama, Gaali mwana wa Ebedi na ndugu zake
wanafika Shekemu; nao wanauchochea mji dhidi yako. 32 Sasa, amka wakati wa

usiku, wewe na askari pamoja nawe, na uandae uvamizi katika mashamba. [33] Kisha
asubuhi, jua litakapokwisha, inuka mapema na uangamize mji. Na yeye na watu
waliokuwa pamoja naye watakapokuja juu yenu, fanyeni chochote mnachoweza.
[34] Basi Abimeleki akainuka usiku, yeye na watu wote waliokuwa pamoja naye,
wakaandaa uvamizi dhidi ya Shekemu, wakagawanyika vitengo vinne. [35] Gaali
mwana wa Ebedi akatoka, akasimama penye mlango wa mji. Abimeleki na watu
waliokuwa pamoja naye wakatoka mahali pa kuficha. [36] Gaali alipowaona hao
watu, akamwambia Zebuli, “Tazama, watu wanatoka kwenye vilima!” Zebuli
akamwambia, “Wewe unaona vivuli juu ya vilima kama vile watu”. [37] Gaali akaongea
tena na kusema, “Angalia, watu wanashuka katikati ya nchi, na kitengo kimoja
kinakuja kwa njia ya mwaloni wa Maenenimu.” [38] Ndipo Zebuli akamwambia, “Je,
maneno yako ya kiburi yako wapi sasa, wewe uliyesema, 'Abimeleki ni nani, ili
tumtumikie?' Je, hao sio watu ambao uliwadharau? Toka sasa na pigana nao.”
[39] Gaali akatoka na alikuwa akiwaongoza watu wa Shekemu, naye alipigana na
Abimeleki. [40] Abimeleki akamfukuza, na Gaali akakimbia mbele yake. Na wengi
wakaanguka na majeraha ya mauti mbele ya mingilio ya lango la mji. [41] Abimeleki
alikaa Aruma. Zebul akawalazimisha Gaal na ndugu zake watoke Shekemu. [42] Siku
ya pili watu wa Shekemu wakatoka shambani, na habari hii ikamfikia Abimeleki.
[43] Aliwachukua watu wake, akawagawanywa katika vitengo vitatu, na wakaandaa
uvamizi mashambani. Aliangalia na kuona watu wakitoka mjini. Akawakamata na
kuwaua. [44] Abimeleki na vitengo vilivyokuwa pamoja naye vilishambulia na kuzuia
maingilio ya lango la mji. Vitengo vingine viwili vilishambulia wote waliokuwa
katika shamba na wakawaua. [45] Abimeleki alipigana na huo mji siku nzima. Aliteka
mji huo, na kuwaua watu waliokuwa ndani yake. Akabomoa kuta za mji na
kueneza chumvi juu yake. [46] Wakati wakuu wote wa mnara wa Shekemu waliposikia
hayo, waliingia katika ngome ya nyumba ya El Berithi. [47] Abimeleki aliambiwa
kuwa viongozi wote walikuwa wamekusanyika pamoja kwenye mnara wa Shekemu.
[48] Abimeleki akaenda mpaka mlima wa Salmoni, yeye na watu wote waliokuwa
pamoja naye. Abimeleki akachukua shoka na kukata matawi. Akaweka juu ya bega
lake na kuwaagiza watu waliokuwa pamoja naye, 'Mlichoona nimekifanya fanyeni
kama nilivyofanya.' [49] Basi kila mmoja akakata matawi, wakamfuata Abimeleki.
Wakayafungia juu ya ukuta wa mnara, nao wakawasha moto, hata watu wote wa
mnara wa Shekemu wakafa, wanaume na wanawake elfu. [50] Abimeleki akaenda
Tebezi, naye akapiga kambi dhidi ya Thebezi, akautwaa. [51] Lakini kulikuwa na
mnara wenye nguvu katika mji, wanaume na wanawake wote na viongozi wote
wa mji walikimbilia na kujifungia wenyewe. Kisha wakaenda juu ya paa la mnara.
[52] Abimeleki alikwenda kwenye mnara na kupigana nao, naye akaenda karibu na
mlango wa mnara ili kuuchoma. [53] Lakini mwanamke akatupa jiwe la juu, juu ya
kichwa cha Abimeleki likavunja fuvu lake. [54] Kisha akamwita yule kijana aliyekuwa
anamchukulia silaha zake, akamwambia, “Chukua upanga wako ukaniue, kwa hiyo
hakuna mtu atakayesema juu yangu, 'Mwanamke alimwua.'” Basi kijana wake
akamchoma naye akafa. [55] Watu wa Israeli walipoona kwamba Abimeleki amekufa,
wakaenda nyumbani. [56] Basi Mungu akalipiza kisasi cha uovu wa Abimeleki
alichomfanyia baba yake kwa kuua ndugu zake sabini. [57] Mungu akafanya uovu
wote wa watu wa Shekemu ugeuke juu ya vichwa vyao wenyewe, na juu yao ilikuja
laana ya Yothamu mwana wa Yerubaali.

# 10

[1] Baada ya Abimeleki, Tola, mwana wa Pua, mwana wa Dodo, mtu wa Isakari,
aliyekaa Shamiri, katika mlima wa Efraimu, akaondoka ili kuwaokoa Israeli. [2] Akawa

mwamuzi wa Israeli miaka ishirini na mitatu. Alikufa na kuzikwa Shamiri.
3 Alifuatiwa na Yairi Mgileadi. Akawa mwamuzi wa Israeli miaka ishirini na miwili.
4 Alikuwa na wana thelathini waliokuwa wakipanda kwenye punda thelathini, na walikuwa na miji thelathini, ambayo inaitwa Hawoth Yairi hata leo, iliyo katika nchi ya Gileadi.
5 Yairi alikufa na kuzikwa Kamoni.
6 Watu wa Israeli waliendelea kutenda maovu mbele za Bwana, wakaabudu Mabaali, Maashtoreti, miungu ya Aramu, miungu ya Sidoni, miungu ya Moabu, miungu ya wana wa Amoni, na miungu ya Wafilisti. Wakamsahau Bwana na hawakamsujudia tena.
7 Hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli, naye akawauza mikononi mwa Wafilisti na katika mikono ya wana wa Amoni.
8 Wakawaangamiza na kuwadhulumu watu wa Israeli mwaka huo, na kwa muda wa miaka kumi na nane waliwafukuza watu wote wa Israeli waliokuwa ng'ambo ya Yordani katika nchi ya Waamori, iliyoko Gileadi.
9 Nao wana wa Amoni wakavuka Yordani, wakapigana na Yuda, na Benyamini, na nyumba ya Efraimu; Israeli akasumbuliwa sana.
10 Ndipo wana wa Israeli wakamwita Bwana, wakisema, “Tumekukosea, kwa sababu tumemwacha Mungu wetu, tukaabudu Mabaali.”
11 Bwana akawaambia wana wa Israeli, “Je, sikuwatoa ninyi kutoka kwa Wamisri, na Waamori, na Waamoni, na Wafilisti,
12 na pia kwa Wasidoni? Waamaleki na Wamaoni walipowakandamiza; mliniita, nami nikawaokoa kutoka katika nguvu zao.
13 Lakini ninyi mliniacha tena na kuabudu miungu mingine. Kwa hiyo, sitawaokoa tena.
14 Nendeni mkaiite miungu mnayoiabudu. Ili iwaokoe wakati wa shida.
15 Wana wa Israeli wakamwambia Bwana, Tumefanya dhambi. Tufanyie chochote kinachoonekana kuwa kizuri kwako. Tafadhali, tuokoe leo.
16 Wakaiacha miungu ya kigeni waliyokuwa nayo, nao wakamwabudu Bwana. Naye akawa na subira juu ya taabu ya Israeli.
17 Ndipo Waamoni wakakusanyika, wakaweka kambi Gileadi. Waisraeli walikutana na kuweka kambi yao huko Mispa.
18 Viongozi wa watu wa Gileadi wakaambiana, 'Ni nani atakayeanza kupigana na Waamoni? Yeye atakuwa kiongozi juu ya wote wanaoishi Gileadi.

# 11

1 Yeftha Mgileadi alikuwa shujaa mwenye nguvu, lakini alikuwa mwana wa kahaba. Gileadi alikuwa baba yake.
2 Mke wa Gileadi pia alizaa wanawe wengine. Wana wa mkewe walipokua, walimlazimisha Yeftha aondoke nyumbani na kumwambia, “Huwezi kurithi chochote kutoka katika familia yetu. Wewe ni mwana wa mwanamke mwingine.”
3 Basi Yeftha akaondoka toka kwa ndugu zake, akaishi katika nchi ya Tobu. Watu wasiokuwa na sheria waliungana na Yeftha na wakaja na kwenda pamoja naye.
4 Siku kadhaa baadaye, wana wa Amoni walipigana na Israeli.
5 Wana wa Amoni walipopigana na Israeli, wazee wa Gileadi wakaenda kumleta Yeftha kutoka nchi ya Tobu.
6 Wakamwambia Yeftha, “Njoo uwe kiongozi wetu ili tupigane na wana wa Amoni.”
7 YEphtha akawaambia viongozi wa Gileadi, “mlinichukia na kunilazimisha kuondoka nyumbani kwa baba yangu. Kwa nini mnakuja kwangu sasa munapokuwa na shida?”
8 Wazee wa Gileadi wakamwambia Yeftha, “Ndiyo sababu tunakugeukia sasa; njoo pamoja nasi pigana na watu wa Amoni, na wewe utakuwa kiongozi juu ya wote wanaoishi Gileadi.
9 Yeftha akawaambia wazee wa Gileadi, “Ikiwa mnanirejesha nyumbani tena ili kupigana na wana wa Amoni, na kama Bwana atatupa ushindi juu yao, nitakuwa kiongozi wenu.”
10 wazee wa Gileadi wakamwambia Yeftha, “Bwana awe shahidi kati yetu ikiwa hatutafanya kama tunavyosema!”
11 Yeftha akaenda pamoja na wazee wa Gileadi, nao watu wakamfanya awe msimamizi na mkuu juu yao. Alipokuwa mbele ya Bwana huko Mizpa, Yeftha akarudia ahadi zote alizozifanya.
12 Ndipo Yeftha akatuma wajumbe kwa mfalme wa wana wa Amoni, akisema, “Ni nini mgogoro huu kati yetu? Kwa

nini umekuja kwa nguvu kuchukua ardhi yetu?” 13 Mfalme wa wana wa Amoni
akawajibu wajumbe wa Yeftha, “Kwa sababu Israeli walipopanda kutoka Misri,
walichukua nchi yangu toka Arnoni hata Yaboki, mpaka Yordani. Sasa rudisha ardhi
hizo kwa amani.” 14 Yefta akatuma tena wajumbe kwa mfalme wa wana wa Amoni,
15 akasema, “Yefita asema hivi, Israeli hawakuchukua nchi ya Moabu na nchi ya
wana wa Amoni; 16 lakini walitoka Misri, na Israeli wakaenda kupitia jangwa hadi
Bahari ya Shamu na Kadeshi. 17 Israeli walipomtuma wajumbe kwa mfalme wa
Edomu, wakisema, 'Tafadhali tunaomba ruhusa tupite katika nchi yako,' mfalme
wa Edomu hakuwasikiliza. Wakawatuma wajumbe kwa mfalme wa Moabu, lakini
akakataa. Basi Israeli wakakaa Kadeshi. 18 Kisha wakapitia jangwani, wakaondoka
katika nchi ya Edomu, na nchi ya Moabu; wakavuka upande wa mashariki wa
nchi ya Moabu, wakapanga ng'ambo ya Arnoni. Lakini hawakuingia mpaka wa
Moabu, maana Arnoni ilikuwa mpaka wa Moabu. 19 Israeli wakatuma wajumbe kwa
Sihoni, mfalme wa Waamori, ambaye alitawala huko Heshboni; Israeli akamwambia,
'Tafadhali, tunaomba tupite katika nchi yako hata mahali petu.' 20 Lakini Sihoni
hakumwamini Israeli apite katika eneo lake. Basi Sihoni akakusanya jeshi lake
lote, akalipeleka Yahasa, na huko akapigana na Israeli 21 Bwana, Mungu wa Israeli,
akamtia Sihoni na watu wake wote mkononi mwa Israeli, nao wakawashinda. Basi
Israeli wakachukua nchi yote ya Waamori waliokaa katika nchi hiyo. 22 Wachukua
kila kitu ndani ya wilaya ya Waamori, kutoka Arnoni hadi Yaboki, na kutoka jangwani
hadi Yordani. 23 Basi, Bwana, Mungu wa Israeli, amewafukuza Waamori mbele ya
watu wake Israeli, na sasa mnataka kuimiliki nchi yao? 24 Je, huwezi kuchukua nchi
ambayo Kemoshi, mungu wako, anakupa? Kwa hiyo nchi yoyote Bwana, Mungu wetu,
ametupa, tutachukua. 25 Sasa wewe ni bora zaidi kuliko Balaki, mwana wa Sipori,
mfalme wa Moabu? Je, alidai kuwa na hoja na Israeli? Je, yeye amewahi kupigana
vita dhidi yao? 26 Wakati Israeli walipoishia miaka mia tatu huko Heshboni na vijiji
vyake, na Aroeri na vijiji vyake, na katika miji yote iliyo karibu na Arnoni, kwa nini
hamkuwachukua tena wakati huo? 27 Sijawafanyia vibaya, lakini mnanifanyia vibaya
kwa kunishambulia. Bwana, mwamuzi, ataamua leo kati ya wana wa Israeli na wana
wa Amoni. 28 Lakini mfalme wa wana wa Amoni akakataa onyo alilotumiwa na
Yeftha. 29 Basi, Roho wa Bwana akamjia Yeftha, akapita Gileadi na Manase, akapitia
Mizpa ya Gileadi, na kutoka Mispa ya Gileadi akapita kwa wana wa Amoni. 30 Yeftha
akaahidi kwa Bwana, akasema, “Ikiwa utanipa ushindi juu ya wana wa Amoni,
31 chochote kinachotoka mlangoni mwa nyumba yangu kunijia mimi nitakaporudi
kwa amani kutoka kwa wana wa Amoni kitakuwa cha Bwana; Nami nitatoa hiyo
sadaka ya kuteketezwa.” 32 Basi Yeftha akapita kwa wana wa Amoni ili kupigana
nao, naye Bwana akampa ushindi. 33 Akawashinda na kusababisha mauaji makubwa
kutoka Aroeri hadi miji ishirini na miwili-na Abeli Keramimu. Basi wana wa Amoni
waliwekwa chini ya uangalizi wa watu wa Israeli. 34 Yeftha alifika nyumbani kwake
huko Mizpa, na binti yake akatoka kumlaki na ngoma na kucheza. Alikuwa mtoto
wake pekee, na badala yake hakuwa na mwana wa kiume wala binti. 35 Mara
tu alipopomwona, alirarua nguo zake akasema, 'Loo! Binti yangu! Umenivunja
kwa huzuni, na umekuwa mtu anayenisababishia maumivu yangu! Kwa maana
nimeapa kwa Bwana, wala siwezi kurudisha ahadi yangu. 36 Akamwambia, “Baba
yangu, umeweka ahadi kwa Bwana, unifanyie kila kitu ulichoahidi; kwa kuwa
Bwana amekulipia kisasi juu ya adui zako, wana wa Amoni.” 37 Akamwambia
baba yake, “Hebu ahadi hii ihifadhiwe kwa ajili yangu. Niache kwa miezi miwili,
nipate kuondoka na kwenda kwenye vilima na kuomboleza juu ya ubikira wangu,
mimi na wenzangu.” 38 Akasema, “Nenda.” Alimtuma kwa muda wa miezi miwili.
Akamwondoa, yeye na wenzake, nao wakauomboleza ubikira wake katika milimani.

39 Mwishoni mwa miezi miwili alirudi kwa baba yake, ambaye alifanya kulingana na
ahadi ya aliyoifanya. Sasa alikuwa hajalala na mwanaume, na ikawa desturi katika
Israeli 40 kwamba binti za Israeli kila mwaka, kwa siku nne, waweze kurejea hadithi
ya binti ya Yeftha Mgileadi.

# 12

1 Watu wa Efraimu walitoka pamoja; nao wakapitia Zafoni, wakamwambia Yeftha,
Kwa nini umetangulia kupigana na wana wa Amoni, wala hukutuita twende pamoja
nawe? Tutachoma nyumba yako. 2 Yeftha akawaambia, Mimi na watu wangu
tulikuwa katika vita kubwa na wana wa Amoni. Nilipokuita, hukuniokoa kutoka
kwao. 3 Nilipoona ya kuwa hamkuniokoa, nikaweka uhai wangu na nguvu yangu
mwenyewe, na kupita kipita ili kupigana na wana wa Amoni, na Bwana alinipa
ushindi. Kwa nini mmekuja kupigana nami leo?" 4 Yeftha akawakusanya watu wote
wa Gileadi na akapigana na Efraimu. Watu wa Gileadi waliwaangamiza wana wa
Efraimu kwa sababu walisema, "Ninyi Wagileadi ni wakimbizi katika Efraimu-katika
Efraimu na Manase." 5 Wagileadi waliteketeza ngome za Yordani zinaelekea Efraimu.
Ikiwa yeyote kati ya waliopona wa Efraimu akisema, Nipe ruhusa niende juu ya
mto; watu wa Gileadi wakamwambia, "Je, wewe ni Mwefraimu?" Ikiwa akasema,
"Hapana," 6 basi watamwambia, Sema Shiboleth. Na kama akisema 'Sibboleth' (kwa
maana hakuweza kutamka neno hilo kwa usahihi), Wagileadi watamkamata na
kumwua kwenye mabwawa ya Yordani. Waefraimu elfu arobaini waliuawa wakati
huo. 7 Yeftha alikuwa mwamuzi juu ya Israeli kwa miaka sita. Ndipo Yeftha Mgileadi
akafa, akazikwa katika moja ya miji ya Gileadi. 8 Baada yake, Ibzani wa Bethlehemu
akawa mwamuzi juu ya Israeli. 9 Alikuwa na wana thelathini. Aliwapeleka binti
thelathini katika ndoa, naye akaleta binti thelathini kutoka nje kwa ajili ya wanawe,.
Alikuwa mwamuzi wa Israeli kwa miaka saba. 10 Ibzani alikufa na kuzikwa huko
Bethlehemu. 11 Baada yake, Eloni wa Zabuloni akawa mwamuzi juu ya Israeli.
Akawaamua Israeli kwa miaka kumi. 12 Eloni wa Zabuloni akafa, akazikwa huko
Aiyaloni katika nchi ya Zabuloni. 13 Baada ya huyo, Abdoni mwana wa Hileli,
Mpirathoni, akawa mwamuzi juu ya Israeli. 14 Alikuwa na wana arobaini na wajukuu
thelathini. Walikuwa wakipanda punda sabini, naye akawaamua Israeli kwa miaka
nane. 15 Abdoni mwana wa Hileli, Mpirathoni, akafa, akazikwa huko Pirathoni katika
nchi ya Efraimu, katika kilima cha Waamaleki.

# 13

1 Watu wa Israeli wakafanya yaliyo mabaya machoni pa Bwana, naye akawatia
mikononi mwa Wafilisti kwa miaka arobaini. 2 Kulikuwa na mtu kutoka Sora, wa
jamaa ya Wadani, jina lake Manoa. Mke wake hakuweza kupata mimba na hivyo
hakuzaa. 3 Malaika wa Bwana akamtokea yule mwanamke akamwambia, Tazame
sasa, umeshindwa kupata mimba, wala hujazaa, lakini utakuwa na mimba na utazaa
mtoto. 4 Sasa kuwa makini usinywe divai au kileo, wala usile kitu chochote kilicho
najisi. 5 Angalia, utakuwa na mjamzito na kuzaliwa mtoto mwanaume. Hakuna
wembe itakayotumiwa juu ya kichwa chake, kwa kuwa mtoto atakuwa Mnaziri
kwa Mungu kutoka tumboni, naye ataanza kuwaokoa Israeli kutoka mkono wa
Wafilisti. 6 Kisha mwanamke akaenda kumwambia mumewe, "Mtu wa Mungu alikuja
kwangu, na kuonekana kwake kulikuwa kama malaika wa Mungu, wa kutisha sana.
Sikumwuliza ametokea wapi, na hakuniambia jina lake. 7 Akaniambia, 'Tazama!
Utakuwa mjamzito, na utazaa mtoto. Basi usinywe divai au kileo, wala usile chakula
chochote ambacho sheria inasema kuwa si safi, kwa kuwa mtoto huyo atakuwa
Mnaziri kwa Mungu tangu akipokuwa tumboni mwako mpaka siku ya kufa kwake."

[8] Ndipo Manoa akamwomba Bwana, akasema, Ee Bwana, tafadhali mruhusu mtu
wa Mungu uliyemtuma arudi kwetu ili atufundishe kile tutakachotendea kwa mtoto
atakayezaliwa hivi karibuni. [9] Mungu akajibu sala ya Manoa, na malaika wa Mungu
akamwendea mwanamke tena akiwa ameketi shambani. Lakini Manoa mumewe
hakuwa pamoja naye. [10] Basi mwanamke akakimbia haraka akamwambia mumewe,
“Tazama! Yule mtu ameonekana kwangu-aliyekuja kwangu siku ile!” [11] Manoa
akasimama na kumfuata mkewe. Alipofika kwa mtu huyo, akasema, “Je, wewe ndiwe
mtu aliyezungumza na mke wangu?'” Mtu huyo akasema, “Ni mimi.” [12] Manoa
akasema, Sasa maneno yako yatimike. Je! kuna maagizo gani kwa ajili ya mtoto,
na kazi yake itakuwa nini? ' [13] Malaika wa Bwana akamwambia Manoa, 'Lazima
mkeo afanye kila kitu nilichomwambia. [14] Asile kitu chochote kinachotokana na
mizabibu, wala usimruhusu kunywa divai au kileo; usimruhusu ale chakula chochote
ambacho sheria inasema kuwa si safi. Anapaswa kutii kila kitu nilichoamuru afanye.
[15] Manoa akamwambia malaika wa Bwana, Tafadhali keti kwa muda, utupe wakati
wa kuandaa mbuzi kwa ajili yako. [16] Malaika wa Bwana akamwambia Manowa, Hata
kama nitakaa, sitakula chakula chako. Lakini ukitayarisha sadaka ya kuteketezwa,
toa kwa Bwana. ' (Manowa hakujua kwamba alikuwa malaika wa Bwana.) [17] Manoa
akamwambia malaika wa Bwana, Jina lako ni nani, ili tukuheshimu wakati maneno
yako yatakapotimia? [18] Malaika wa Bwana akamwambia, Mbona unauliza jina langu?
Ni ajabu! ' [19] Manoa akamchukua huyo mbuzi pamoja na sadaka ya nafaka, akatoa
sadaka juu ya mwamba kwa Bwana. Alifanya jambo la ajabu wakati Manoah na mke
wake walikuwa wakiangalia. [20] Wakati huo moto ukatoka juu ya madhabahu kwenda
mbinguni, malaika wa Bwana akapanda katika moto wa madhabahu. Manoah
na mkewe waliona jambo hilo wakainamisha vichwa vyao chini. [21] malaika wa
Bwana hakuonekana tena kwa Manoa au mkewe. Manoa akajua kwamba yule ndiye
malaika wa Bwana. [22] Manoa akamwambia mkewe, 'Hakika tutakufa, kwa sababu
tumemwona Mungu!' [23] Lakini mkewe akamwambia, Ikiwa Bwana alitaka kutuua,
asingepokea sadaka ya kuteketezwa na sadaka ya nafaka tuliyompa. Asingetuonesha
mambo haya yote, wala wakati huu asingeweza kuturuhusu tusikie mambo hayo.
[24] Baadaye mwanamke akamzaa mtoto, akamwita jina lake Samsoni. Mtoto alikua
na Bwana akambariki. [25] Roho wa Bwana akaanza kumchochea Mahane Dani, kati
ya Sora na Eshtaoli.

# 14

[1] Samsoni akashuka kwenda Timna, na huko akaona mwanamke, mmojawapo wa
binti za Wafilisti. Aliporudi, akamwambia baba yake na mama yake, [2] 'Nimemwona
mwanamke huko Timna, mmojawapo wa binti za Wafilisti. Sasa mkanichukulie awe
mke wangu. [3] Baba yake na mama yake wakamwambia, “Je, hakuna mwanamke
kati ya binti za ndugu zako, au kati ya watu wetu wote? Je! Utachukua mke
kutoka kwa Wafilisti wasiotahiriwa?” Samsoni akamwambia baba yake, “Nichukulie
kwa ajili yangu, kwa maana wakati nilipomwangalia, alinipendeza.' [4] Lakini baba
yake na mama yake hawakujua kwamba suala hili lilikuja kutoka kwa Bwana, kwa
maana alitaka kutengeneza mgogoro na Wafilisti (kwa wakati huo Wafilisti walikuwa
wakitawala Israeli). [5] Basi Samsoni akaenda Timna pamoja na baba yake na mama
yake; nao wakafika kwenye mashamba ya mizabibu ya Timna. Na, tazama, kuna
simba mdogo wa alikuja na alikuwa akiunguruma. [6] Roho wa Bwana ghafla akaja
juu yake, naye akamrarua simba kwa urahisi kama ambavyo angeweza kumrarua
mbuzi mdogo, naye hakuwa na kitu mkononi mwake. Lakini hakuwaambia baba
au mama yake kile alichofanya. [7] Alikwenda na kuzungumza na mwanamke, na
alipopomtazama, alimpendeza Samsoni. [8] Siku chache baadaye aliporudi kumwoa,

akageuka na kutafuta mzoga wa simba. Na, tazama, kulikuwa na kundi la nyuki
na asali katika kile kilichobaki katika mwili wa simba. 9 Akaweka asali mikononi
mwake na akaenda, akala huku akienda. Alipokuja kwa baba yake na mama yake,
akawapa, nao wakala. Lakini hakuwaambia kuwa amechukua asali nje ya kile
kilichobaki kwenye mwili wa simba. 10 Baba yake Samsoni akaenda chini alipokuwa
mwanamke, na Samsoni akafanya sikukuu huko, kwa maana hii ilikuwa desturi
ya vijana. 11 Mara tu ndugu zake walipomwona, walimletea rafiki zao thelathini
kuwa pamoja naye. 12 Samsoni akawaambia, Hebu nawaambieni kitendawili. Ikiwa
mmoja wenu anaweza kuipata na kuniambia jibu wakati wa siku saba za sikukuu,
nitatoa nguo za kitani thelathini na seti ya nguo thelathini. 13 Lakini ikiwa hamuwezi
kuniambia jibu, basi utanipa nguo za kitani thelathini na seti za nguo thelathini. '
Wakamwambia, Utuambie kitendawili chako, ili tukisikie. 14 Akawaambia, 'Kati ya
mtu aliyekula alikuwa kitu cha kula; nje ya nguvu ilikuwa kitu tamu. Lakini wageni
wake hawakuweza kupata jibu katika siku tatu. 15 Siku ya nne wakamwambia mkewe
Samsoni, 'Mdanganye mume wako ili atuambie jibu la kitendawili, au tutakuchoma
moto wewe na nyumba ya baba yako. Je, umetualika hapa ili kutufanya maskini?
' 16 Mke wa Samsoni alianza kulia mbele yake; Akasema, 'Yote unayoyafanya ni
kunichukia! Hunipendi. Umesema kitendawili kwa baadhi ya watu wangu, lakini
hujawaambia jibu. ' Samsoni akamwambia, 'Angalia hapa, kama sijawaambia baba
yangu au mama yangu, nikuambie wewe?' 17 Alilia kwa siku saba ambazosikukuu
yao iliendelea. Siku ya saba alimwambia jibu kwa sababu alimlazimisha sana.
Akawaambia jibu jamaa zake. 18 Na watu wa mji wakamwambia, siku ya saba
kabla ya jua kuzama, 'Ni nini kilicho bora zaidi kuliko asali? Ni kitu gani chenye
nguvu kuliko simba? ' Samsoni akawaambia, 'Ikiwa hamkulima na ng'ombe wangu,
hamtapata jibu la kitendawili changu.' 19 Kisha Roho wa Bwana akaja kwa Samsoni
kwa nguvu. Samsoni akashuka kwenda Ashkeloni na kuuawa watu thelathini kati ya
watu hao. Akachukua mateka yao, na akawapa seti ya nguo kwa wale waliomjibu
kitendawili chake. Alikasirika akaenda nyumbani kwa baba yake. 20 Na mke wake
akachukuliwa na rafiki yake wa karibu.

# 15

1 Baada ya siku kadhaa, wakati wa mavuno ya ngano, Samsoni akachukua mbuzi
mdogo akaenda kumtembelea mkewe. Akajiambia mwenyewe, “Nitaenda kwenye
chumba cha mke wangu.” Lakini baba yake hakumruhusu aingie. 2 Baba yake
akasema, “Nilidhani umemchukia, hivyo nikampatia rafiki yako. Dada yake mdogo
ni mzuri kuliko yeye, Mchukue badala yake.” 3 Samsoni akawaambia, 'Wakati huu
sitakuwa na hatia juu ya Wafilisti wakati nikiwaumiza.' 4 Samsoni akaenda na
kukamata mbweha mia tatu akawafunga pamoja kila jozi, mkia hadi mkia. Kisha
akachukua taa na kuzifunga katikati ya kila mkia. 5 Alipokwisha kuviwasha moto
vienge, akawaachia mbweha katika nafaka za Wafilisti zilizosimama, nao wakawasha
moto nafaka zote zilizopandwa, na nafaka iliyosimama shambani, pamoja na
mashamba ya mizabibu na mizeituni. 6 Wafilisti waliuliza, “Ni nani aliyefanya
hili?” Wakaambiwa, “Samsoni, mkwe wa Mtimna alifanya hivyo kwa sababu Mtimna
alimchukua mke wa Samsoni akampa rafiki yake.” Basi Wafilisti wakamwendea
wakamchoma kwa moto yeye na baba yake. 7 Samsoni akawaambia, “Ikiwa ndivyo
mnavyofanya, nitalipiza kisasi juu yenu, na baada ya hayo, nitaacha.” 8 Kisha
akawakata vipande vipande, paja na mguu, kwa kuwauwa sana. Kisha akashuka
chini akaishi katika pango katika mwamba wa Etamu. 9 Ndipo Wafilisti wakaja,
wakajitahidi kupigana vita huko Yuda, wakaanzisha jeshi lao huko Lehi. 10 Watu
wa Yuda wakasema, “Kwa nini mmekuja kutupiga?” Wakasema, “Tunashambulia

ili tuweze kumkamata Samsoni, na tumtendee kama alivyotutendea.” [11] Kisha
watu elfu tatu wa Yuda wakashuka hata kwenye pango la Eatamu, wakamwambia
Samsoni, “Je, hujui kwamba Wafilisti hutawala juu yetu? Je! umetutendea
nini?” Samsoni akawaambia, “Kwa kadili walivyonitendea mimi, vivyo hivyo
nimewatendea wao.” [12] Wakamwambia Samsoni, “Tumeshuka kukufunga na kukutia
mikononi mwa Wafilisti.” Samsoni akawaambia, “Niapieni kwamba hamtaniua ninyi
wenyewe.” [13] Wakamwambia, “La, tutakufunga tu kwa kamba na kukupeleka kwao.
Tunakuahidi sisi hatutakuua.” Kisha wakamfunga na kamba mbili mpya na kumleta
kutoka kwenye mwamba. [14] Alipofika Lehi, Wafilisti walipiga kelele walipokutana
naye. Kisha Roho wa Bwana akaja juu yake kwa nguvu. Kamba zilizokuwa juu
ya mikono yake zikawa kama kitambaa cha kuteketezwa, na zikaanguka mikononi
mwake. [15] Samsoni alipata mfupa mbichi wa taya ya punda, naye akaichukua na
kuua watu elfu kwa mfupa huo. [16] Samsoni akasema, “Kwa taya ya punda, chungu
juu ya chungu, na njaa ya punda nimewaua watu elfu.” [17] Samsoni alipomaliza
kuzungumza, akatupa taya, na akaita mahali pale Ramath Lehi. [18] Samsoni alikuwa
na kiu sana akamwita Bwana na kusema, “Umempa mtumishi wako ushindi mkubwa.
Lakini sasa nitakufa kwa kiu na kuanguka mikononi mwa wale wasiootahiriwa?”
[19] Na Mungu akapafungua mahali pa shimo palipo katika Lehi, na maji yakatoka.
Alipokunywa, nguvu zake zikarejea na akahuishwa. Kwa hiyo aliita jina la mahali
hapo Enhakore, na ni huko Lehi hadi leo. [20] Samsoni alikuwa mwamuzi wa Israeli
katika siku za Wafilisti kwa miaka ishirini.

# 16

[1] Samsoni alikwenda Gaza na akamwona kahaba huko, naye akalala pamoja
naye. [2] Watu wa Gaza wakaambiwa, “Samsoni amekuja hapa.” Watu wa Gaza
wakazunguka mahali hapo kwa siri, wakamngoja usiku wote katika lango la jiji.
Walikaa kimya usiku wote. Wakisema, “Hebu tusubiri mpaka mchana, na kisha
tumwuue.” [3] Samsoni akalala kitandani mpaka usiku wa manane. Usiku wa manane
akaamka na akashika mlango wa jiji na miimo yake miwili. Akavivuta kutoka nje,
komeo na vyote, akaviweka kwenye mabega yake, akavichukua hadi juu ya kilima,
mbele ya Hebroni. [4] Baada ya hayo, Samsoni alimpenda mwanamke aliyeishi katika
bonde la Soreki. Jina lake alikuwa Delila. [5] Wale wakuu wa Wafilisti wakamwendea,
wakamwambia, “mdanganye Samsoni ili uone mahali zilipo nguvu zake kuu, na kwa
namna gani tunaweza kumshinda, ili tumfunge na kumtesa. Fanya hili, na kila mmoja
wetu atakupa vipande 1, 100 vya fedha.” [6] Ndipo Delila akamwambia Samsoni,
“Tafadhali, niambie ni kwa jinsi gani wewe ni mwenye nguvu sana, na kwa namna
gani mtu anaweza kukufunga, ili aweze kukudhibiti?” [7] Samsoni akamwambia,
“Ikiwa watanifunga na kamba saba safi ambazo hazijakauka, nitakuwa dhaifu na
kuwa kama mtu mwingine yeyote.” [8] Basi wakuu wa Wafilisti wakamletea Delila
kamba saba ambazo hazijakauka, naye akamfunga Samsoni. [9] Sasa alikuwa na
watu waliojificha kwa siri, walikaa katika chumba chake cha ndani. Akamwambia,
“Wafilisti wako juu yako, Samsoni!” Lakini akazikata kamba kama uzi wakati
unapogusa moto. Na hawakujifunza siri ya nguvu zake. [10] Ndipo Delila akamwambia
Samsoni, “Ndivyo ulivyonidanganya mimi na kuniambia uongo. Tafadhali, niambie
kwa namna gani unaweza kufungwa.” [11] Akamwambia, “Ikiwa watanifunga na
kamba mpya ambayo haijawahi kutumika kwa kazi, nitakuwa dhaifu na kama mtu
mwingine yeyote.” [12] Basi Delila alichukua kamba mpya akamfunga pamoja naye,
akamwambia, “Wafilisti wako juu yako Samsoni!” Watu waliokuwa wakisubiri
walikuwa ndani ya chumba cha ndani. Lakini Samsoni akaondoa kamba kutoka
mikono yake kama kilikuwa kipande cha uzi. [13] Delila akamwambia Samsoni, “Mpaka

sasa umenidanganya na kuniambia uongo. Niambie kwa namna gani unaweza
kufungwa.” Samsoni akamwambia, 'Ikiwa utavifuma vifungo saba vya nywele zangu
na kuvifunga kwenye kitambaa, kisha kufunga kwenye msumari, nitakuwa kama mtu
mwingine yeyote.” 14 Alipokuwa amelala, Dalila akavifuma vifungo saba vya nywele
zake akavifunga ndani ya kitambaa na kuzifunga kwenye msumari, akamwambia,
“Wafilisti wako juu yako, Samsoni!” Aliamka kutoka usingizini akang'oa kitambaa
na pini zilizokuwa zimefungwa. 15 Akamwambia, “Wawezaje kusema,” Unanipenda,
wakati hushiriki siri zako na mimi? Umenidhihaki mara tatu hizi na hukukuambia
ni kwa jinsi gani unazo nguvu nyingi.” 16 Kila siku alisisitiza kwa bidii na
maneno yake, naye akamkemea sana kiasi kwamba alitamani kufa. 17 Basi Samsoni
alimwambia kila kitu, akamwambia, “Wembe haujawahi kukata nywele juu ya
kichwa changu, kwa maana nimekuwa Mnaziri kwa Mungu kutoka tumboni mwa
mama yangu. Ikiwa kichwa changu kitanyolewa, basi nguvu zangu zitaniacha,
nami nitakuwa dhaifu na kuwa kama kila mtu mwingine. ' 18 Delila alipoona
kwamba amemwambia ukweli juu ya kila kitu, akawatuma na kuwaita watawala
wa Wafilisti, akisema, “Njooni tena, kwa maana ameniambia kila kitu.” Ndipo
wakuu wa Wafilisti wakamwendea, wakaleta fedha mkononi mwao. 19 Alimfanya
alale katika magoti yake. Alimwita mtu avinyoe vifungo saba vya kichwa chake,
naye akaanza kumshinda, kwa maana nguvu zake zilikuwa zimemwacha. 20 Alisema,
“Wafilisti wako juu yako, Samsoni!” Aliamka nje ya usingizi wake akasema, “Nitatoka
nje kama nyakati nyingine na kujiweka huru.” Lakini hakujua kwamba Bwana
amemwacha. 21 Wafilisti walimkamata na kumng'oa macho. Wakampeleka Gaza
na kumfunga kwa shaba. Alikuwa akisaga ngano katika gerezani. 22 Lakini
nywele juu ya kichwa chake zilianza kukua tena baada ya kunyolewa. 23 Watawala
wa Wafilisti walikusanyika ili kutoa dhabihu kubwa kwa Dagoni mungu wao, na
kufurahi. Walisema, “mungu wetu amemshinda Samsoni, adui yetu, na kumtia
katika ufahamu wetu.” 24 Watu walipomwona, walimsifu mungu wao, kwa sababu
walisema, “mungu wetu ameshinda adui yetu na kutupa sisi - mharibifu wa nchi yetu,
ambaye aliwaua wengi wetu.” 25 Walipokuwa wakisherehekea, wakasema, 'Mwite
Samsoni, aje kutufurahisha.' Walimwita Samsoni nje ya jela na akawafanya wacheke.
Walimsimamisha katikati ya nguzo. 26 Samsoni akamwambia yule kijana ambaye
alikuwa ameshika mkono wake, 'Niruhusu nishike nguzo zilizoshikilia nyumba hii,
ili nipate kuegemea.” 27 Sasa nyumba ilikuwa imejaa wanaume na wanawake.
Watawala wote wa Wafilisti walikuwa huko. Juu ya paa kulikuwa na wanaume
na wanawake elfu tatu, ambao walikuwa wakiangalia wakati Samsoni alipokuwa
akiwafurahisha. 28 Samsoni akamwita Bwana, akasema, “Bwana MUNGU, nipe nia!
Tafadhali niimarishe mara moja tu, Mungu, ili nipate kulipiza kisasi kwa Wafilisti
kwa kuchukua macho yangu mawili. 29 Samsoni aliweka nguzo mbili katikati ambzo
zinashikilia nyumba hiyo, naye akaegemea juu yake, nguzo moja kwa mkono wake
wa kuume, na mwingine kwa kushoto kwake. 30 Samsoni akasema, “Na nife pamoja
na Wafilisti!” Alipanda kwa nguvu zake na jengo likaanguka juu ya watawala na juu
ya watu wote waliokuwa ndani yake. Hivyo waliouawa wakati alikufa walikuwa zaidi
ya wale waliouawa wakati wa maisha yake. 31 Kisha ndugu zake na nyumba yote ya
baba yake wakashuka. Wakamchukua, wakamrudisha na kumzika kati ya Sora na
Eshtaoli katika mahali pa kuzikwa Manoa, baba yake. Samsoni alikuwa mwamuzi
wa Israeli kwa miaka ishirini.

## 17

1 Kulikuwa na mtu katika nchi ya vilima ya Efraimu, na jina lake ni Mika.
2 Akamwambia mama yake, “Shilingi 1, 100 za fedha ambazo zilichukuliwa kutoka

kwako, ambazo ulizungumza kwa kiapo, na kuniambia-tazama hapa! Ninazo fedha
pamoja nami. Nimeziiba." Mama yake akasema, 'Na Bwana atakubariki, mwanangu!'
3 Alirejesha vipande 1, 100 vya fedha kwa mama yake na mama yake akasema,
"Nimeweka fedha hii kwa Bwana, kwa ajili ya mwanangu kuifanya na kuchonga
takwimu za chuma. 4 Kwa hiyo sasa, ninawarejesha." Alipokuwa amrudishia
mama yake fedha, mama yake alichukua vipande mia mbili za fedha na akawapa
mfanyakazi wa chuma ambaye aliwafanya kuwa sanamu na kuchonga takwimu za
chuma, na wakawekwa ndani ya nyumba ya Mika. 5 Mtu huyo Mika alikuwa na
nyumba ya sanamu, naye akafanya efodi na nyumba ya miungu, naye akaajiri mmoja
wa wanawe awe mkuhani wake. 6 Siku hizo hapakuwa na mfalme huko Israeli, na
kila mtu alifanya yaliyo sawa machoni pake. 7 Kisha kulikuwa na kijana mmoja wa
Bethlehemu huko Yuda, wa jamaa ya Yuda, ambaye alikuwa Mlawi. Alikaa huko
ili kutimiza majukumu yake. 8 Mtu huyo aliondoka Bethlehemu huko Yuda kwenda
kutafuta mahali pa kuishi. Alipokuwa akienda, afika nyumbani kwa Mika katika nchi
ya mlima wa Efraimu. 9 Mika akamwambia, Unatoka wapi? Huyo mtu akamwambia,
Mimi ni Mlawi wa Bethlehemu huko Yuda, ninakwenda kutafuta mahali nipate
kuishi. 10 Mika akamwambia, "kaa pamoja nami, uwe baba yangu na kuhani wangu.
Nitawapa vipande kumi vya fedha kwa mwaka, suti ya nguo, na chakula chako." Basi
Mlawi akaingia nyumbani mwake. 11 Mlawi alikuwa na furaha ya kuishi na mtu huyo,
na huyo kijana kwa Mika akawa kama mmoja wa wanawe. 12 Mika akamtenga Mlawi
kwa ajili ya kazi takatifu, na huyo kijana akawa kuhani wake, naye alikuwa katika
nyumba ya Mika. 13 Ndipo Mika akasema, Sasa najua ya kuwa Bwana atanifanyia
mema, kwa kuwa Mlawi huyu amekuwa kuhani wangu.

# 18

1 Siku hizo hapakuwa na mfalme huko Israeli. Kabila la Wadani lilikuwa linatafuta
makazi ya kuishi, kwa maana mpaka siku hiyo hawakupokea urithi wowote kutoka
miongoni mwa makabila ya Israeli. 2 Watu wa Dani walituma watu watano kutoka
kwa idadi yote ya kabila lao, wanaume wenye ujasiri kutoka Sora na kutoka Eshtaoi,
ili kukagua ardhi kwa miguu, na kuiangalia. Wakawaambia, "Nendeni mkaangalie
nchi.' Wakafika nchi ya mlima wa Efraimu, kwa nyumba ya Mika wakalala huko.
3 Walipokuwa karibu na nyumba ya Mika, walitambua maneno ya Mlawi. Basi
wakamsimama na kumwuliza, "Nani alikuleta hapa? Unafanya nini hapa? Kwa
nini uko hapa?" 4 Akawaambia, "Hivi ndivyo Mika amefanya kwa ajili yangu Yeye
aliniajiri mimi kuwa kahani wake." 5 Wakamwambia, "Tafadhali tafuta ushauri
kwa Mungu, ili tuweze kujua kama safari tunayoendea itafanikiwa." 6 Kuhani huyo
akawaambia, "Nenda kwa amani. Bwana atakuongoza katika njia unayoiendea."
7 Kisha wale watu watano wakaondoka na wakafika Laishia, na waliona watu
waliokuwa pale waliishi salama- vivyo hivyo Wasidoni waliishi bila kusumbuliwa na
kwa usalama. Hapakuwa na mtu aliyewashinda katika nchi hiyo, au aliyewasumbua
kwa namna yoyote. Waliishi mbali na Wasidoni, na hawakuwa na ushirikiano na
mtu yeyote. 8 Walirudi kwa kabila lao huko Zora na Eshtaol. Ndugu zao waliwauliza,
'Mna habari gani?' 9 Wakasema, "Njoo! Hebu tuwashambulie! Tumeona ardhi na
ni nzuri sana. Je hamfanyi kitu? Msiwe wavivu kushambulia na kuchukua ardhi.
10 Mnapoenda, mtakuta watu wanaofikiri wapo salama, na nchi ni pana! Mungu
amewapa ninyi-mahali ambako hapajapungukiwa kitu chochote duniani. ' 11 Watu
mia sita wa kabila la Dani, wenye silaha za vita, waliondoka kutoka Sora na Eshtaoli.
12 Wakasafiri, wakapanga Kiriath-yearimu, huko Yuda. Ndio maana watu walipaita
mahali pale Mahane Dani hata leo; ni magharibi ya Kiriath yearimu. 13 Wakaondoka
huko na kwenda nchi ya mlima wa Efraimu, wakafika nyumbani kwa Mika. 14 Kisha

watu watano waliokuwa wamekwenda kutazama nchi ya Laisha waliwaambia jamaa
zao, “Je, mnajua kwamba katika nyumba hizi kuna efodi, miungu ya kaya, sanamu
zilizochongwa, na sanamu za chuma? Amua sasa utakachofanya.” 15 Basi wakarudi
huko, wakafika nyumbani mwa Mlawi, nyumbani mwa Mika; wakamsalimu. 16 Wana
Daniani mia sita, wenye silaha za vita, walisimama kwenye maingilio ya lango.
17 Wale watu watano waliokuwa wamekwenda kutembelea nchi walikwenda huko
na wakachukua sanamu zilizochongwa, efodi, na miungu ya nyumba, na sanamu
ya chuma, wakati kuhani alipokuwa amesimama kwenye maingilio ya lango na
wanaume mia sita wenye silaha za vita. 18 Walipokuwa wakiingia nyumbani kwa
Mika na kuchukua sanamu zilizochongwa, efodi, miungu ya nyumba, na sanamu
za chuma, kuhani akasema, “mnafanya nini?” 19 Wakamwambia, “Tulia! Weka
mkono wako kwenye kinywa chako na uje nasi, na uwe kwetu baba na kuhani. Je,
ni bora kuwa wewe kuhani kwa ajili ya nyumba ya mtu mmoja, au kuhani kwa
kabila na jamaa katika Israeli?” 20 Moyo wa kuhani ulifurahi. Akachukua efodi,
miungu ya nyumba, na sanamu ya kuchongwa, akaenda pamoja na hao watu. 21 Basi
wakageuka wakaenda. Wameweka watoto wadogo mbele yao wenyewe, pamoja na
ng'ombe na mali zao. 22 Walipokuwa umbali mzuri kutoka kwa nyumba ya Mika,
watu waliokuwa ndani ya nyumba iliyo karibu na nyumba ya Mika waliitwa, nao
wakawafikia Wadani. 23 Waliwapigia kelele Wadani, nao wakageuka, wakamwambia
Mika, “Kwa nini mmekuja pamoja? 24 Akasema, “ninyi mmeiba miungu niliyoifanya,
mmemchukua kuhani wangu, na mnaondoka. Je, nina nini tena? Unawezaje
kuniuliza, 'Ni nini kinachokusumbua?'” 25 'Watu wa Dani wakamwambia,” Usiruhusu
tusikie chochote unachosema, au baadhi ya watu wenye hasira sana watawapiga,
wewe na familia yako mtauawa.” 26 Ndipo watu wa Dani wakaenda zao. Mika
alipoona kwamba walikuwa na nguvu sana juu yake, akageuka na kurudi nyumbani
kwake. 27 Watu wa Dani walichukua kile alichokifanya Mika, pamoja na kuhani
wake, na wakafika Laisha, kwa watu waliokuwa hawasumbuliwi na wenye usalama
na salama wakawaua kwa upanga na kuuchoma mji huo. 28 Hapakuwa na mtu wa
kuwaokoa kwa sababu palikuwa na umbali mrefu kutoka Sidoni, na hawakuwa na
uhusiano na mtu yeyote. Palikuwa katika bonde lililo karibu na Beth Rehobu. Wadani
wakaujenga mji na kuishi huko. 29 Wakauita jina lake Dani, jina la baba zao Dani,
ambaye alikuwa mmoja wa wana wa Israeli. Lakini jina la mji hapo mwanzo ulikuwa
Laisha. 30 Watu wa Dani walijenga sanamu za kuchonga wenyewe. Naye Yonathani,
mwana wa Gershomu, mwana wa Musa, yeye na wanawe walikuwa makuhani wa
kabila la Wadani mpaka siku ya uhamisho wa nchi. 31 Basi wakaiabudu sanamu ya
kuchonga ya Mika aliyoifanya wakati wa nyumba ya Mungu huko Shilo.

# 19

1 Katika siku hizo, wakati hakuna mfalme katika Israeli, kulikuwa na mtu, Mlawi,
aliyekuwa akiishi kwa muda kidogo katika eneo la mbali zaidi ya nchi ya Efraimu.
Alijichukulia mwanamke, masuria kutoka Bethlehemu huko Yuda. 2 Lakini mkewe
hakuwa mwaminifu kwake; akaondoka na kurudi nyumbani kwa baba yake huko
Bethlehemu ya Yuda. Alikaa huko kwa muda wa miezi minne. 3 Kisha mumewe
akaondoka na kumfuata ili kumshawishi arudi. Mtumishi wake alikuwa pamoja
naye, na punda wawili. Akamleta nyumbani kwa baba yake. Baba wa msichana
alipomwona, alifurahi. 4 Baba mkwe wake, baba wa msichana, alimshawishi kukaa
siku tatu. Walikula na kunywa, na walikaa usiku huko. 5 Siku ya nne waliamka
mapema na alijiandaa kuondoka, lakini baba wa msichana akamwambia mkwewe,
“Jipe nguvu na mkate kidogo, kisha unaweza kwenda.” 6 Basi hao wawili wakaketi
kula na kunywa pamoja. Kisha baba ya msichana akasema, “Tafadhali uwe tayari

kukaa usiku huu na kuwa na wakati mzuri.' 7 Mlawi alipoinuka ili aondoke, baba wa
mwanamke huyo alimwomba akae, hivyo alibadili mpango wake na akalala usiku
tena. 8 Siku ya tano aliamka mapema kuondoka, lakini baba wa msichana akasema,
'Jitie nguvu mwenyewe, na kusubiri mpaka alasiri.' Kwa hiyo hao wawili wakala
chakula. 9 Mlawi na suria wake na mtumishi wake wakainuka ili kuondoka, baba
mkwe wake, baba wa msichana akamwambia, “Angalia, sasa mchana unaelekea
jioni. Tafadhali kaa usiku mwingine, na uwe na wakati mzuri. Unaweza kuamka
kesho mapema na kurudi nyumbani.” 10 Lakini Mlawi hakuwa tayari kukaa usiku.
Aliamka na kuondoka. Akaenda kuelekea Yebusi (hiyo ni Yerusalemu). Alikuwa
na pande mbili za punda-na masuria wake alikuwa pamoja naye. 11 Walipokuwa
karibu na Yebusi, siku hiyo ilikuwa imeenda mno, na mtumishi akamwambia bwana
wake, Haya, tupate kwenda kwa mji wa Wayebusi, tukakae ndani yake usiku huu.
12 Bwana wake akamwambia, “Hatuwezi kwenda katika mji wa wageni ambao si
wa wana wa Israeli.” Tutakwenda Gibea. 13 Mlawi akamwambia yule kijana,
“Njoo, twende sehemu moja wapo, na tukae usiku huko Gibea au Rama.” 14 Basi,
wakaenda, na jua likachwea wakiwa karibu na Gibea, katika eneo la Benyamini.
15 Wakageuka huko ili wawezenkukaa usiku huko Gibea. Naye akaingia na kukaa
katika njia kuu ya jiji, maana hakuna mtu aliyewaingiza nyumbani kwake usiku.
16 Lakini mtu mzee alikuwa akija kutoka kazini kwake katika shamba jioni hiyo.
Alikuwa kutoka mlima wa Efraimu, naye alikuwa akikaa kwa muda huko Gibea.
Lakini watu wanaoishi mahali hapo walikuwa Wabenyamini. 17 Aliinua macho na
kumwona msafiri katika njia kuu ya jiji. Huyo mzee akasema, “Unakwenda wapi?
Unatoka wapi?” 18 Mlawi akamwambia, “Tunaenda kutoka Betelehemu ya Yuda
mpaka sehemu ya mbali zaidi ya nchi ya kilima ya Efraimu, ambako mimi hutoka.
Nilikwenda Bethlehemu huko Yuda, nami nenda nyumbani mwa Bwana; lakini
hakuna mtu atakayenichukua nyumbani kwake. 19 Tuna nyasi za kulisha punda zetu,
na kuna mkate na divai kwa ajili yangu na mtumishi wako mwanamke hapa, na kwa
kijana huyu pamoja na watumishi wako. Hatujapungukiwa chochote. ' 20 Huyo mzee
akawasalimu, “Amani iwe na wewe! Nitakupatia mahitaji yako yote. Usikae usiku
tu katika njia kuu.” 21 Basi huyo mtu akamleta Mlawi nyumbani kwake, akawalisha
punda. Wakaosha miguu yao na kula na kunywa. 22 Walipokuwa wakifurahisha
mioyo yao, watu wengine wa jiji, watu wasiokuwa na maana, walizunguka nyumba,
wakipiga mlango. Wakamwambia yule mzee, mwenye nyumba, wakisema, “Mtoe
mtu aliyeingia nyumbani kwako, ili tuweze kufanya mapenzi naye.” 23 Yule mtu,
mwenye nyumba, akawajia, akawaambia, “Hapana, ndugu zangu, tafadhali msifanye
jambo baya! Kwa kuwa mtu huyu ni mgeni nyumbani kwangu, musifanye jambo
hili baya!” 24 Angalia, binti yangu bikira na masuria wake hawa hapa. Ngoja
niwalete sasa. Wapuuze na kufanya nao chochote mnachopenda. Lakini msifanyie
jambo hili mbaya kwa mtu huyu!” 25 Lakini watu hawakumsikiliza, kwa hiyo huyo
mwanamume akamshika yule mwanamke, akamleta nje. Walimkamata, wakambaka,
na kumtendea uovu usiku mzima, na asubuhi wakamruhusu aende. 26 Asubuhi
mwanamke alikuja akaanguka chini ya mlango wa nyumba ya mtu ambapo bwana
wake alikuwa, na yeye akalala pale mpaka kulipokucha. 27 Bwana wake akaondoka
asubuhi na kufungua milango ya nyumba, akatoka kwenda njiani. Aliweza kumwona
mwanamke wake amelala pale mlangoni, mikono yake ikiwa juu ya kizingiti. 28 Mlawi
akamwambia, “Simama twende.” Lakini hakujibiwa. Alimuweka juu ya punda, na
huyo mtu akaondoka nyumbani. 29 Mlawi alipofika nyumbani kwake, akachukua
kisu, naye akamshika suria wake, akamkataa, mguu kwa mguu, akafanya vipande
kumi na viwili, akapeleka vipande kila mahali katika Israeli. 30 Wote waliona hili
wakasema, “Kitu hicho hakijawahi kufanyika au kuonekana tangu siku ambayo watu

wa Israeli walikuja kutoka nchi ya Misri mpaka leo. Fikiria juu ya hili! Tupe ushauri!
Tuambie nini cha kufanya!”

# 20

[1] Ndipo watu wote wa Israeli wakatoka kama mtu mmoja, toka Dani mpaka Beer-
sheba, pamoja na nchi ya Gileadi; nao wakakusanyika mbele za Bwana huko Mispa.
[2] Viongozi wa watu wote, wa kabila zote za Israeli, wakachukua nafasi zao kwenye
kusanyiko la watu wa Mungu-watu 400, 000 waendao kwa miguu, ambao walikuwa
tayari kupigana na upanga. [3] Basi wana wa Benyamini waliposikia kwamba watu
wa Israeli walikuwa wamepanda Mispa. Wana wa Israeli wakasema, “Tuambieni
ni kwa namna gani huu uovu umefanyika.” [4] Mlawi, mume wa mwanamke
aliyeuawa, akajibu, Nilikuja Gibea katika nchi ya Benyamini, mimi na suria wangu,
ili tulale. [5] Wakati wa usiku, viongozi wa Gibea walinishambulia, wakizunguka
nyumba na wakakusudia kuniua. Walimkamata na kumbaka suria wangu, naye
akafa. [6] Nilimchukua suria wangu na kumkata mwili wake vipande vipande, na
kuweka katika kila nchi ya urithi wa Israeli, kwa sababu wamefanya uovu huo na
upumbavu katika Israeli. [7] Sasa, ninyi Waisraeli wote, toeni maneno na ushauri
wenu hapa.” [8] Watu wote wakaondoka pamoja kama mtu mmoja, wakasema,
Hakuna hata mmoja wetu atakayeenda hemani kwake, wala hakuna hata mmoja
wetu atakayerudi nyumbani kwake. [9] Lakini sasa hivi ndivyo tutakavyoifanyia Gibea
tutaishambulia kama kura inavyotuongoza. [10] Tutachukua watu kumi katika mia
moja katika makabila yote ya Israeli, na mia moja katika elfu, na elfu moja katika
elfu kumi, kuwapa chakula kwa ajili ya watu hawa, ili waweze kufika Gibea katika
Benyamini, watawaadhibu kwa uovu wao waliofanya katika Israeli. [11] Basi askari
wote wa Israeli wakakusanyika juu ya mji, kama mtu mmoja. [12] Makabila ya Israeli
waliwatuma watu kwa kabila lote la Benyamini, wakisema, “Uovu huu uliofanywa
kati yenu ni nini? [13] Kwa hiyo, tupeni watu hao waovu wa Gibea, tupate kuwaua,
na hivyo tutaondoa kabisa uovu huu kutoka kwa Israeli.” Lakini Wabenyamini
hawakusikiliza sauti ya ndugu zao, watu wa Israeli, [14] Ndipo wana wa Benyamini
wakakusanyika kutoka mijini kwenda Gibea, wakajiandaa kupigana na wana wa
Israeli. [15] Watu wa Benyamini wakakusanya kutoka miji yao ili kupigana siku
ile, askari elfu ishirini na sita waliopangwa kupigana na upanga. Walakini, kuna
watu mia saba waliochaguliwa kutoka kwa wenyeji wa Gibea. [16] Miongoni mwa
askari wote hawa walikuwa watu mia saba waliochaguliwa ambao walikuwa wenye
shoto. Kila mmoja wao angeweza kupiga unywele kwa mawe na asikose. [17] Watu
wa Israeli, bila kuhesabu namba kutoka kwa Benyamini, walikuwa na watu 400,
000 waliokuwa wamejifunza kupigana na upanga. Wote hawa walikuwa watu wa
vita. [18] Watu wa Israeli waliondoka, wakaenda Betheli, wakaomba ushauri kutoka
kwa Mungu. Wakauliza, “Ni nani kwanza atakayewaangamiza watu wa Benyamini
kwa ajili yetu?” Bwana akasema, “Yuda atashambulia kwanza.” [19] Watu wa Israeli
waliamka asubuhi na wakahamisha kambi yao karibu na Gibea. [20] Watu wa Israeli
walikwenda kupigana na Benyamini. Wakaweka nafasi zao za vita dhidi yao huko
Gibea. [21] Watu wa Benyamini wakatoka Gibea, nao wakawaua watu elfu ishirini
na mbili wa jeshi la Israeli siku ile. [22] Wana wa Israeli walijitia nguvu wenyewe,
na wakaunda mstari wa vita mahali pale walipokwisha kuchukua nafasi siku ya
kwanza. [23] Na wana wa Israeli wakaenda, wakalia mbele za Bwana hata jioni.
Walitaka mwongozo kutoka kwa Bwana “Je, tunapaswa kwenda tena kupigana na
ndugu zetu, watu wa Benyamini?” Naye Bwana akasema, “Wapigeni!” [24] Basi
watu wa Israeli wakapigana na askari wa Benyamini siku ya pili. [25] Siku ya pili,
Benyamini alitoka kupigana nao kutoka Gibea, nao wakawaua watu wa Israeli elfu

kumi na nane. Wote walikuwa watu ambao walijifunza kupigana na upanga. [26] Basi
askari wote wa Israeli na watu wote wakaenda Betheli, wakalia, wakakaa mbele
za Bwana; nao wakafunga siku hiyo hata jioni, wakatoa sadaka za kuteketezwa
na sadaka za amani mbele za Bwana. [27] Wana wa Israeli wakamwomba Bwana,
- kwa sababu ya sanduku la agano la Mungu lilikuwapo siku hizo; [28] na Finehasi,
mwana wa Eleazari, mwana wa Haruni, aliyekuwa akihudumia mbele ya sanduku
siku hizo. "Je twende vitani tena dhidi ya watu wa Benyamini, ndugu zetu, au
tuache?" Bwana akasema, "Wapigeni, kwa maana kesho nitawasaidia kuwashinda.
[29] Basi Israeli akaweka watu mahali pa siri karibu na Gibea. [30] Watu wa Israeli
wakapigana na wana wa Benyamini kwa siku ya tatu, nao wakajenga vita vyao
juu ya Gibea, kama walivyotangulia. [31] Watu wa Benyamini wakaenda kupigana na
watu, nao wakachukuliwa mbali na mji. Walianza kuua baadhi ya watu. Kulikuwa
na watu thelathini wa Israeli ambao walikufa katika mashamba na barabara. Njia
moja ilienda Betheli, na nyingine ikaenda Gibea. [32] Ndipo wana wa Benyamini
wakasema, "Wameshindwa na wanatukimbia, kama hapo awali." Lakini askari
wa Israeli wakasema, "Hebu tukimbie na kuwavuta mbali na mji hadi barabarani."
[33] Watu wote wa Israeli waliondoka kutoka mahali pao na wakajipanga kwa vita huko
Baal-Tamari. Basi askari wa Israeli waliokuwa wakijificha mahali pa siri walikimbia
kutoka Maare-Geba. [34] Wakatoka juu ya Gibea watu kumi elfu waliochaguliwa
kutoka Israeli yote, na vita vilikuwa kali, lakini Wabenjamini hawakujua kwamba
msiba ulikuwa karibu nao. [35] Bwana akamshinda Benyamini mbele ya Israeli.
Siku hiyo, askari wa Israeli waliwauawa watu wa Benyamini 25, 100. Wote hawa
waliokufa walikuwa wale waliokuwa wamejifunza kupigana na upanga. [36] Basi
askari wa Benyamini waliona wameshindwa. Wana wa Israeli walikuwa wametoa
ardhi kwa Benyamini, kwa kuwa walikuwa wakihesabu watu waliowaweka katika
nafasi zilizofichwa nje ya Gibea. [37] Ndipo watu waliokuwa wameficha wakainuka na
haraka na wakamkimbia Gibea. Nao wakauawa kila mtu aliyeishi mjini kwa upanga
wao. [38] Ishara iliyopangwa kati ya askari wa Israeli na watu waliojificha kwa siri
itakuwa wingu kubwa la moshi litatokea nje ya mji. [39] Ishara ilipokuja askari wa
Israeli wakageuka kutoka kwenye vita. Basi Benyamini wakaanza kushambulia na
wakawaua watu wa Israeli thelathini, wakasema, "Hakika wanapigwa mbele yetu,
kama katika vita vya kwanza." [40] Lakini wakati nguzo ya moshi ilipoanza kuinuka
nje ya mji, Wabenjamini waligeuka na kuona moshi ukitanda mbinguni kutoka mji
mzima. [41] Ndipo watu wa Israeli wakawageuka. Wana wa Benyamini waliogopa, kwa
sababu waliona kwamba maafa yaliwajia. [42] Basi wakakimbia kutoka kwa wana wa
Israeli, kuelekea njia ya jangwani. Lakini vita viliwapata. Askari wa Israeli walitoka
mijini na wakawaua pale waliposimama. [43] Waliwalzungukia wana wa Benjamini
na wakawafuata. Nao wakawakanyaga huko Noha, wakawaua mpaka upande wa
mashariki wa Gibea. [44] Kutoka kabila la Benyamini, watu kumi na nane elfu walikufa,
wote walikuwa wanaume waliojulikana katika vita. [45] Wakageuka na kukimbia
kuelekea jangwani hadi mwamba wa Rimoni. Waisraeli waliuawa zaidi ya elfu
tano kati yao barabarani. Waliendelea kuwafuata, wakifuata kwa njia kuu kwenda
Gidomu, na huko waliuawa elfu mbili zaidi. [46] Askari wote wa Benyamini walioshuka
siku hiyo walikuwa watu ishirini na tano waliokuwa wamejifunza kupigana kwa
upanga; wote walikuwa wanajulikana katika vita. [47] Lakini watu mia sita wakageuka
na kukimbilia jangwani, kuelekea mwamba wa Rimoni. Wakakaa katika mwamba
wa Rimoni kwa muda wa miezi minne. [48] Askari wa Israeli waliwarudia watu
wa Benyamini na wakawashinda na kuwaua-mji mzima, ng'ombe, na kila kitu
walichopata. Pia walichoma moto kila mji katika njia yao.

# 21

1 Sasa watu wa Israeli walikuwa wameahidi huko Mispa, “Hakuna hata mmoja wetu
atakayempa binti yake kuolewa na Mbenyamini.” 2 Ndipo watu wakaenda Betheli,
wakakaa huko mbele ya Mungu hata jioni; wakalia kwa sauti kubwa. 3 Walipiga
kelele, “Kwa nini, Bwana, Mungu wa Israeli, amefanya jambo hili kwa Waisraeli,
kwamba moja ya makabila yetu linapotea leo?” 4 Siku iliyofuata watu waliamka
mapema na wakajenga madhabahu huko na kutoa sadaka za kuteketezwa na sadaka
za amani. 5 Watu wa Israeli wakasema, “Ni nani kati ya kabila zote za Israeli
hawakuja katika mkutano wa Bwana?” Kwa kuwa walikuwa wamefanya ahadi
muhimu juu ya mtu yeyote ambaye hakuja kwa Bwana huko Mispa. Wakasema,
“Hakika yeye atauawa.” 6 Watu wa Israeli walikuwa na huruma kwa ndugu yao
Benyamini. Wakasema, “Leo hii kabila moja limekatiliwa mbali kutoka Israeli.
7 Ni nani atakayewapa wale walioachwa wake, kwa kuwa tumeahidi kwa Bwana
kwamba hatuwezi kuwaruhusu yeyote kati yao aoe binti zetu?” 8 Wakasema, “Ni
nani kati ya kabila za Israeli hawakuja kwa Bwana huko Mispa? Ilionekana kuwa
hakuna mtu aliyekuja kwenye mkusanyiko kutoka Jabeshi-Gileadi. 9 Kwa maana
watu walipokuwa wamepangwa kwa utaratibu, tazama, hakuna hata mmoja wa
wenyeji wa Yabeshi Gileadi. 10 Mkutano huo uliwatuma watu kumi na wawili wa
watu wao wenye ujasiri kwa maagizo ya kwenda Jabeshi-gileadi na kuwaangamiza,
na kuwaua, hata wanawake na watoto. 11 “Fanya hivi unapaswa kuua kila mume
na kila mwanamke aliyelala na mwanaume.” 12 Watu wale walikuta watu kati ya
hao waliokaa Yabeshi-gileadi, wanawake mia nne ambao hawakulala na mwanaume,
wakawapeleka kwenye kambi huko Shilo, huko Kanaani. 13 Mkutano wote ukatuma
ujumbe na kuwaambia watu wa Benyamini waliokuwa kwenye mwamba wa Rimoni
kwamba walikuwa wanawapa amani. 14 Wabenyamini walirudi wakati huo na
walipewa wanawake wa Yabeshi Gileadi, lakini hapakuwa na wanawake wa kutosha
kwa wote. 15 Watu waliomboleza kwa kile kilichotokea Benyamini, kwa kuwa Bwana
alifanya mgawanyiko kati ya makabila ya Israeli. 16 Kisha wakuu wa mkutano
wakasema, “Tutafanyaje ili Wabenyamini wapate wake, kwa kuwa wanawake wa
Benyamini wameuawa?” 17 Wakasema, 'Lazima kuwe na urithi kwa Wabenyamini
waliosalia, ili kabila lisiharibiwe kutoka Israeli. 18 Hatuwezi kuwapa wake kutoka
kwa binti zetu, kwa kuwa wana wa Israeli walikuwa wametoa ahadi, 'Na alaaniwe
mtu atakayempa Benyamini mke.'” 19 Wakasema, “Mnajua kuwa kuna sikukuu
kwa Bwana kila mwaka huko Shilo ( ambayo ni kaskazini ya Betheli, mashariki
ya barabara inayopanda kutoka Betheli hadi Shekemu, na kusini mwa Lebona).
20 Wakawaagiza wana wa Benyamini, wakisema, “Nendeni, mjifiche kwa siri, na
kusubiri katika mashamba ya mizabibu. 21 Tazama wakati ambapo wasichana
kutoka Shilo watatoka kucheza, Tokeni nje ya mizabibu na kila mmoja wenu
anapaswa kunyakua mke kutoka kwa wasichana wa Shilo, kisha kurudi kwenye
nchi ya Benyamini. 22 Wakati baba zao au ndugu zao watakapokuja kutupinga,
tutawaambia, 'Tupeni neema! Waache wabaki kwa sababu hatukupata wake kwa
kila mtu wakati wa vita. Na ninyi hamna hatia juu ya ahadi, kwa sababu hamkuwapa
wao binti zenu.'” 23 Watu wa Benyamini walifanya hivyo. Walichukua idadi ya wake
waliowahitaji kutoka kwa wasichana waliokuwa wakicheza, nao wakawachukua ili
wawe wake zao. Wakaenda na kurudi mahali pa urithi wao; wakajenga tena miji,
na wakaishi ndani yao. 24 Kisha watu wa Israeli wakatoka mahali hapo na kwenda
nyumbani, kila mmoja kwa kabila lake na ukoo, na kila mmoja kwa urithi wake
mwenyewe. 25 Siku hizo hapakuwa na mfalme huko Israeli. Kila mtu alifanya yaliyo
sawa machoni pake mwenyewe.

# Ruth

[1] Ilitokea katika siku za utawala wa majaji kuwa kulikuwa na njaa katika nchi, na
mtu mmoja wa Bethelehemu ya Yuda alikwenda katika nchi ya Moabu pamoja na
mke wake na watoto wake walili wa kiume. [2] Jina la mtu huyo lilikuwa Elimeleki,
na jina la mke wake lilikuwa Naomi. Majina ya watoto wake wawili wa kiume
waliitwa Mahiloni na Kileoni, ambao walikuwa Waefraimu wa Betherehemu ya Yuda.
Waliwasili katika nchi ya Moabu na kuishi hapo. [3] Ndipo Elimeleki, mume wa Naomi,
alikufa, na Naomi aliachwa na watoto wake wa kiume wawili. [4] Watoto hawa walioa
wanawake wa Moabu; jina la mmoja lilikuwa Oripa, na jina la mwingine lilikuwa
Ruth. waliishi huko kwa takribani miaka kumi. [5] Kisha wote Mahiloni na Kileoni
walikufa, na kumuacha Naomi bila mme wake na bila watoto wake wawili. [6] Ndipo
Naomi aliamua kuondoka Moabu pamoja na wake wa watoto wake na kurudi Yuda
kwa sababu alikuwa amesikia katika mkoa wa Moabu kuwa Yahweh amewasaidia
watu wake katika uhitaji na amewapa chakula. [7] Hivyo aliondoka sehemu aliyokuwa
pamoja na wake wa watoto wake wawili, walitelemka njia kurudi kwenye nchi ya
Yuda. [8] Naomi aliwaambia wake wa watoto wake, “Nendeni, mrudi, kila mmoja
wenu, kwenye nyumba ya mama yake. na Mungu aonyeshe wema juu yenu, kama
mlivyo onyesha wema kwao waliokufa na kwangu. [9] Mungu awajalie ninyi kupata
pumziko, kila mmoja wenu katika nyumba ya mme mwingine.” Kisha akawabusu, na
wakapaza sauti zao na kulia. [10] Wakamwambia, “Hapana! tutarudi pamoja na wewe
kwa watu wako.” [11] Lakini Naomi alisema, “Rudini, wanangu! Kwa nini mtakwenda
na mimi? Kwani bado nina watoto katika tumbo langu kwa ajili yenu, ili kwamba
waje wawe waume zenu? [12] Rudini, wanangu, nendeni katika njia zenu wenyewe,
kwa kuwa mimi ni mzee sana kuwa na mme. Kama nikisema, 'Natumaini nipate
mume usiku huu,' na kisha kuzaa watoto wakiume, kwa hiyo mnaweza kusubiri
mpaka wakue? [13] Mtasubiri na msiolewe sasa? Hapana, wanangu! Ina nihuzunisha
zaidi, kuliko inavyo wahuzunisha ninyi, kwa sababu mkono wa Yahweh umeenda
kinyume na mimi.” [14] Ndipo wake wa watoto wake wakapaza sauti zao na kulia
tena. Oripa alimuaga kwa kumbusu, lakini Ruth aliendelea kubaki naye. [15] Naomi
alisema, “sikiliza, mwenzako amerudi kwa watu wake na miungu yake. Ruri pamoja
naye.” [16] lakini Ruth alisema, “Usiniache niondoke mbali nawe, kwa kuwa uendako,
nitakwenda, utakapoishi, nitaishi; watu wako watakuwa watu wangu, na Mungu
wako atakuwa Mungu wangu. [17] Mahali utakapofia, nitafia hapo, na hapo nitazikwa.
Yahweh aniwezeshe, na hata zaidi, ikiwa kuna chochote isipokuwa kifo kamwe
hakiwezi kututenganisha. [18] Naomi alipoona kuwa Ruth alikuwa ameamua kwenda
naye, aliacha kubishana naye. [19] Hivyo wote wawili walisafiri mpaka walipofika
mjini Bethelehemu. Kwa hiyo walipofika Bethlehemu, mji wote uliwafurahia,
wanawake walisema, “Huyu ni Naomi?” [20] Lakini aliwaambia, “Msiniite Naomi.
Niiteni Mchungu, kwa kuwa Mwenyezi Mungu amenitenda mambo machungu sana.
[21] Nilikwenda nikiwa nimejaa, lakini Yahweh kanirudisha nyumbani nikiwa sina
wote. Hivyo kwa nini mnaniita Naomi, wakati mnaona Yahweh amenihukumu,
kuwa Mwenyezi Mungu amenitaabisha?” [22] Kwa hivyo Naomi na Ruth Mmoabu,
mke wa mtoto wake, walirudi kutoka nchi ya Moabu. walirudi Bethrehemu mwazo
wa mavuno ya shairi.

## 2

[1] Basi Elimeleki mme wa Naomi, alikuwa na jamaa aitwaye Boazi, aliye kuwa
tajiri, na mtu maarufu. [2] Ruth, Mmoabu, alimwambia Naomi, “Ngoja niende

nikakusanye mabaki ya chakula katika shamba. Nitamfuata yeyote ambaye nitapata
kibali machoni pake.” Hivyo naomi akamwambia, “Nenda, mwanangu.” 3 Ruth
alienda kuvuna kwenye shamba akiwafuata kwa nyuma wavunaji. Na kumbe ile
sehemu ya shamba ilikuwa ni mali ya Boazi, aliyekuwa na mahusiano na Elimeleki.
4 Tazama, Boazi alikuja kutoka bethelehemu na kuwaambia wavunaji, “Yahweh awe
nanyi.” Wakamjibu, “Yahweh akubariki.” 5 Ndipo Boazi akamwambia mtumishi
wake aliyekuwa akiwasimamia wavunaji, “Vipi bwana huyu msichana ni wa nani?”
6 Mtumishi msimamizi wa wavunaji alijibu na kusema, “Ni msichana Mmoabu
aliyerudi na Naomi kutoka nchi ya Moabu. 7 Aliniambia, 'Tafadhali niruhusu kuvuna
na kukusanya mabaki ya wavunaji.' Hivyo alikuja na ameendelea kuvuna toka
asubuhi mpaka sasa, isipokuwa amepumzika kidogo katika nyumba.” 8 Kisha Boazi
akamwambia Ruth, “Unanisikiliza, mwanangu? Usiende kuvuna kwenye shamba
lingine; usiondoke shambani kwangu. Badala yake, baki hapa na wasichana wangu
wa kazi. 9 Yaelekeze tu macho yako kwenye shamba ambamo wanaume wanavuna
na ufuatie nyuma ya wanawake wengine. Je, sikuwaelekeza wanaume wasikuguse?
Na upatapo kiu, unaweza kwenda kunywa maji kwenye mtungi ambao wanaume
wamejaza.” 10 Ndipo akapiga magoti mbele ya Boazi, na kugusisha kichwa chake
chini. Akamwambia, “Kwa nini nimepata kibali machoni pako, hata unijali mimi
mgeni?” 11 Boazi akajibu na kumwabia, “Nimekwisha ambiwa, yote uliyo yafanya
tangu mme wako afariki. Umewaacha baba yako, mama, na nchi uliyozaliwa
kumfuata mama mkwe wako na kuja kwa watu usiowajua. 12 Yahweh akulipe kwa
matendo yako. Yahweh akulipe kwa wingi, Mungu wa Israeli, ambaye chini ya
mbawa zake umepata kimbilio.” 13 Ruth akasema, “Nipate kibali machoni pako,
bwana wangu, kwa kuwa umenifariji, na umeongea wema kwangu, ingawa mimi
sio mmoja wa watumishi wako wa kike.” 14 Wakati wa chakula Boazi alimwambia
Ruth, “Njoo hapa, ule baadhi ya mikate, na uchovye kipande katika divai.” Alikaa
kando ya wavunaji, na Boazi akampatia kiasi cha nafaka zilizo kaangwa. Ruth
alikula mpaka alipotosheka na kusaza. 15 Alipoinuka kwenda kuvuna, Boazi aliamuru
vijana wake, akisema, “Mwacheni avune hata katika masuke, na msimwambie lolote
baya. 16 Na pia muachie baadhi ya masuke katika vifurushi kwa ajili yake, na
muaache ili ayavune. Msimkemee.” 17 Kwa hiyo alivuna mpaka jioni. Kisha
akatenganisha nafaka na majani ambayo amevuna, nazo nafaka zilikuwa kama
efa moja ya shairi. 18 Akazibeba na kwenda katika mji. Ndipo mama mkwe
wake aliona kile alichokivuna. Ruth pia alimletea mama mkwe wake nafaka zilizo
kaangwa alizobakiza kwenye chakula chake. 19 Mama mkwe wake akamwambia,
“Umevunia wapi uliko vunia leo? Ulienda kufanyia wapi kazi? abarikiwe mtu
aliye kusaidia.” Ndipo Ruth akamwambia mama mkwe wake kuhusu mtu aliye
miliki shamba alilokuwa akifanya kazi. Alimwambia, “Jina la mtu ambaye alimiliki
shamba nililokuwa nikifanya kazi ni Boazi.” 20 Naomi akamwambia Ruth, “Abarikiwe
na Yahweh, ambaye hakuondoa uaminifu wake kwa walio hai na wafu.” Naomi
akamwambia, “Huyo mtu ni jamaa wa karibu nasi, ni jamaa yetu mkombozi.”
21 Ruth Mmoabu akamwambia, “Ni kweli, aliniambia, 'Ukae karibu na vijana wangu
wa kiume mpaka watakapo maliza mavuno yangu yote.'” 22 Naomi akamwambia
Ruth mke wa mtoto wake wa kiume, “Ni vizuri, mwanangu, kuwa uende pamoja
na wasichana wake wa kazi, ili kwamba usije pata madhara yeyote katika shamba
lolote.” 23 Kwa hiyo alikaa karibu na wafanyakazi wa kike ili avune mpaka mwisho
wa mavuno ya shayiri na mavuno ya ngano. Na alikuwa akiishi pamoja na mama
mkwe wake.

# 3

1 Naomi, mama mkwe wake, alimwambia, “Mwanangu, hainilazimu kutafuta
mahali pa wewe kupumzika, ili kwamba mambo yako yaende vizuri? 2 Naye Boazi,
mtu ambaye umekuwa pamoja na wasichana wake wa kazi, yeye si jamaa yetu?
Tazama, jioni hii atakuwa akikung'uta shairi katika sakafu ya kupuria. 3 Kwa hiyo,
oga, jipake mafuta, uvae nguo zako nzuri, na ushuke kwenda kwenye sakafu ya
kupuria. Lakini usijulikane kwa mtu huyu mpaka atakapo maliza kula na kunywa.
4 Na uhakikishe kuwa, atakapo lala chini, ukumbuke mahali alipo lala ili kwamba
baadaye uende kwake, ufunue miguu yake, na ulale hapo. Kisha atakuambia cha
kufanya.” 5 Ruth alimwambia Naomi, “Nitafanya kila kitu ulicho sema.” 6 Alishuka
kwenda kwenye sakafu ya kupuria, na alifuata maelekezo aliyopewa na mama mkwe
wake. 7 Boazi alipomaliza kula na kunywa na moyo wake ulikuwa na furaha, alienda
kulala chini mwisho wa sehemu ya kuhifadhia nafaka. Kisha Ruth akaenda taratibu,
akaaifunua miguu ya Boazi, na kulala hapo chini. 8 Panapo usiku wa manane Boazi
alisituka. Akajigeuza, na hapo mwanamke alikuwa amelala katika miguu yake!
9 Akamwambia, “Wewe ni nani?” Akajibu, “Mimi ni Ruth, mtumishi wako wa kike.
Nifunike shuka lako mimi mtumishi wako wa kike, kwa kuwa wewe ni jamaa wa
karibu.” 10 Boazi akamwambia, “Mwanangu, Yahweh akubariki. Umeonyesha wema
mwishoni kuliko mwazoni, kwa sababu hukwenda kwa wanaume vijana, awe tajiri
au masikini. 11 Na sasa, mwanangu, usiogope! Nitakufanyia yote unayosema, kwa
sababu mji wa watu wangu wote wanajua kuwa wewe ni mwanamke unayestahili.
12 Nikweli kuwa mimi ni jamaa wa karibu; hata hivyo, kuna jamaa wa karibu kuliko
mimi. 13 Baki hapa usiku huu, na asubuhi, ikiwa atafanya jukumu lake la jamaa
wa karibu, vizuri, muache afanye jukumu lake la kindugu. lakini kama hata fanya
jukumu la kindugu kwako, ndipo mimi nitafanya, kama Yahweh aishivyo. Lala
mpaka asubuhi.” 14 Kwa hiyo Ruth alilala kwenye miguu ya Boazi hadi asubuhi.
Lakini aliamka mapema kabla ya yeyote kuweza kumtambua mtu mwingine. Kwa
kuwa alikwisha mwambia, “Isijulikane kuwa mwanamke alikuja kwenye sakafu ya
kupuria.” 15 Kisha Boazi akamwambia, lete mtandio wako na uushikilie.” Alipo
fanya hivyo, alipima vipimo vikubwa sita vya shairi katika mtandio na kumtwisha
Ruth. Kisha Boazi akaenda mjini. 16 Ruth aliporudi kwa mama mkwe wake, alisema,
“Ulifanyaje, mwanangu?” Ndipo Ruth akamwambia mambo yote aliyotendewa na
mtu huyo. 17 Alimwambia, “Hivi vipimo sita vya shairi ni vile alivyonipa yeye, kwa
kuwa alisema, 'Usiende mikono mitupu kwa mama mkwe wako.'” 18 Kisha Naomi
akasema, “Baki hapa, mwanangu, mpaka utakapojua yatakavyo kuwa, kwa kuwa
Boazi hata pumzika mpaka atakapolimaliza jambo hili leo.”

# 4

1 Ndipo Boazi akaenda kwenye lango la Bethelehemu na kukaa chini. Muda mfupi
tu akaja ndugu wa karibu ambaye Boazi alimuongelea. Boazi akamwambia, “Rafiki
yangu, njoo hapa na uketi. Kisha mtu huyo akaja na kuketi. 2 Ndipo Boazi akakusanya
viongozi kumi wa mji na kusema, “Katini hapa.” Hivyo wakaketi. 3 Boazi alimwambia
yule jamaa wa karibu, “Naomi aliyerudi kutoka mji wa Moabu, anauza sehemu ya
aridhi ambayo ilikuwa ni miliki ya kaka yetu Elimeleki. 4 Nilifikiria kukujulisha na
kukwambia, 'Inunue mbele ya hawa waliokaa hapa, na mbele ya viongozi wa watu
wangu.' Ikiwa utapenda kuikomboa, ikomboe. Lakini ikiwa hauhitaji kuikomboa,
uniambie, ili nijue, kwa kuwa hakuna mwingine wa kuikomboa isipokuwa wewe,
na mimi ni mdogo wako.” Ndipo huyo mtu mwingine akasema, “Nitalikomboa.”
5 Kisha Boazi akasema, “Ile siku utakayonunua shamba kutoka mkononi mwa Naomi,
yakupasa pia kumchukua Ruth Mmoabu, mjane wa mtoto wa Elimeleki, ili kuliinua

jina la marehemu kama urithi wake.” 6 Ndipo yule jamaa wa karibu akasema, “Mimi
siwezi kuikomboa ardhi kwa ajili yangu bila kuleta athari kwenye urithi wangu
binafsi. Nakupa wewe haki ya kuikomboa kwa ajili yako mwenyewe, kwa kuwa
mimi sitoweza.” 7 Hii ilikuwa ni desturi ya zamani ya Israeli kuhusu ukombozi na
kubadilishana mazuri. Kudhibitisha mambo haya yote, mtu huyu alivua kiatu chake
na kumpatia jirani yake; hii ilikuwa ni namna ya kufanya makubaliano ya kisheria
katika Israeli. 8 Kwa hiyo huyu jamaa wa karibu akamwambia Boazi, “Inunue
mwenyewe.” Kisha akavua kiatu chake. 9 Ndipo Boazi akawaambia viongozi na
watu wote, “Ninyi ni mashaidi kuwa nimenunua kila kilichokuwa cha Elimeleki na
kila kilichokuwa na Kileoni na Mahilon kutoka kwenye mikono ya Naomi. 10 Zaidi
ya hayo kumhusu Ruth Mmoabu, mke wa Mahlon: nimempa kibali cha kuwa mke
wangu, ili kuendeleza jina na urithi wa marehumu, ili kwamba jina lake lisipotee
kati ya ndugu zake na lango la watu wake. Ninyi ni mashahidi leo.” 11 Watu wote
na viongozi waliokuwa katika lango, walisema, “Tu mashahidi. Yahweh amfanye
mwanamke huyu ambaye amekuja nyumbani kwako kama Raheli na Leya, ambao
wawili hawa wameijenga nyumba ya Israeli. Na ubarikiwe katika Efrata na kuwa
mashuhuri katika Bethelehem. 12 Na nyumba yako kama nyumba ya Peres, ambaye
Tamari alimzalia yuda, kupitia uzao ambao Yahweh atakupatia pamoja na msichana
huyu.” 13 Hivyo Boazi alimchukua Ruth, na akawa mke wake. Boazi alilala naye,
na Yahweh alimruhusu kupata mimba, na alizaa mtoto wa kiume. 14 Wanamke
huyu akamwambia Naomi, “Yahweh abarikiwe, ambaye hajakuacha bila ndugu wa
karibu, yaani mtoto huyu. Jina lake na liwe maarufu katika Israeli. 15 Na awe
kwako mrutubishaji wa maisha na mwenye ruzuku uzeeni mwako, kwa kuwa mtoto
wako mkwe, ambaye anakupenda, ambaye ni bora kwako kuliko watoto wa kiume
saba, amemzaa. 16 Kisha naomi akamchukua mtoto, akamlaza kifuani pake, na
kumhudumia. 17 Na majirani wa yule mwanamke, wakampa jina, wakisema, “Mtoto
amezaliwa kwa Naomi.” Wakawita Obedi. Ambaye alikuja kuwa baba yake na Jese,
ambaye alikuja kuwa baba yake na Daudi. 18 Hiki kilikuwa ni kizazi cha Peresi: Peres
alimzaa Hezroni, 19 Hezroni akamzaa Ram, Ram akamzaa Aminadabu, 20 Aminadabu
akamzaa Nashon, Nashon akamzaa Salmon, 21 Salmon akamzaa Boazi, Boazi akamzaa
Obed, 22 Obedi akamzaa Jese, na Jese akamzaa Daudi.

# 1Samweli

1 Palikuwa na mtu mmoja wa Rama Msufi, wa nchi ya milima milima ya Efraimu;
jina lake aliitwa Elikana mwana Yerohamu mwana Elihu mwana wa Tohu mwana
wa Sufu, Mwefraimu. 2 Mtu huyo alioa wanawake wawili, jina la mke wa kwanza
aliitwa Hana, na yule wa pili aliitwa Penina, Penina alizaa watoto, lakini Hana
hakuzaa. 3 Kila mwaka, mtu huyu aliondoka mjini kwake kwenda kuabudu na
kutoa dhabihu kwa BWANA wa majeshi huko Shilo. Wana wawili wa Eli, Hofni na
Finehasi, makuhani wa BWANA, walikuwepo huko Shilo. 4 Kila mwaka zamu ya
Elikana ya kutoa dhabihu ilipofika, alikuwa daima akimpa sehemu ya nyama Penina
mkewe, watoto wake wote wa kiume na wakike 5 Lakini kwa mgawo wa Hana daima
alimpa mara mbili zaidi, kwa sababu alimpenda Hana, ingawa BWANA alikuwa
amelifunga tumbo lake. 6 Hasimu wake alimchokoza sana ili kumkasilisha, kwa
sababu BWANA alikuwa amelifunga tumbo lake. 8 7 Hivyo kila mwaka, alipokuwa
akienda katika nyumba ya BWANA pamoja na familia yake, hasimu wake alizidi
kumchokoza, Hatimaye alikuwa mtu wa kulia kila wakati na hakula kitu chochote.
8 Elikana mmewe kila wakati alimuuliza, “Hana, kwa nini unalia? Kwa nini huli
chakula? Kwa nini una huzuni moyoni mwako? Mimi sibora kwako kuliko wana
kumi? 9 Wakati fulani, walipokuwa wamemaliza kula na kunywa huko Shilo, Hana
alinyanyuka. Wakati huo Eli, kuhani alikuwa amekaa juu ya kiti chake mlangoni
kuelekea nyumba ya BWANA. 10 Hana alijawa na uchungu sana; akamwomba BWANA
na akalia mno. 11 Aliweka nadhili na kusema, “BWANA wa majeshi, kama utalitazama
teso la mjakazi wako na kunikumbuka, na usipomsahau mjakazi wako, na kumpatia
mjakazi wako mtoto wa kiume, ndipo nitamtoa huyo mtoto kwa BWANA siku zote za
maisha yake, na wembe hautapita juu ya kichwa chake kamwe”. 12 Hana kiendelea
kuomba mbele za BWANA, Eli alikitazama kinywa chake. 13 Hana aliongea moyoni
mwake. Midomo yake ilitikisika, lakini sauti yake haikusikika. Hivyo Eli alimdhania
kuwa amelewa. 14 Eli akamwambia, “Utakuwa mlevi mpaka lini? Weka mbali divai
yako.” 15 Hana akajibu, “Sivyo bwana wangu, mimi ni mwanamke mwenye roho
ya huzuni. Sijanywa divai wala kinywaji chochote cha kulevya, bali nimekuwa
nikiimimina nafsi yangu mbele za BWANA.” 16 Usimchukulie mjakazi wako kama
mwanamke duni; nimekuwa nikiongea kutokana na maumivu na masikitiko yangu.”
18 17 Kisha Eli alimjibu na kusema, “Nenda kwa amani; na Mungu wa Israeli akupatie
kile ulichomuomba.” 18 Hana akasema, “ Na mjakazi wako apate kibali machoni
pako.” Ndipo huyo mwanamke alienda zake na kula chakula na hakuhuzunika
tena. 19 Waliamka asubuhi na mapema wakaenda wakamtukuza BWANA, na baadaye
walirudi nyumbani kwao Rama. Elikana alilala na mke wake Hana, na BWANA
akamkumbuka. 20 Baada ya muda fulani, Hana alibeba mimba na akazaa mtoto
wa kiume. Akamwita jina lake Samweli, akasema, “Kwa sababu huyu nilimuomba
kutoka kwa BWANA.” 21 Mara nyingine, Elikana na nyumba yake, walipanda kwenda
kumtolea BWANA dhabihu ya Mwaka na kuondoa nadhiri yake. 22 Lakini Hana
hakwenda huko; alikuwa amekwisha mwambia mmewe, “Sitaenda huko hadi mtoto
aache kunyonya; ndipo nitamleta, ili ahudhurie mbele za BWANA na akae huko
daima.” 23 Mme wake Hana, Elikana, akamwambia, “Fanya yale yakupendezayo.
Ngojea hadi utakapokuwa umemwachisha kunyonya; BWANA aweze peke yake
kuthibitisha neno lake.” Hivyo yule mwanamke alibaki akimnyonyesha mtoto
wake mpaka pale alipomwachisha ziwa. 24 Alipokuwa amemwachisha kunyonya,
alimbeba, akimchukua pamoja ng'ombe dume wa miaka mitatu, unga kama kilo

thelathini na chupa ya mvinyo, akampeleka katika nyumba ya BWANA huko Shilo.
Na mtoto huyo alikuwa bado mdogo. [25] Walimchinja yule ng'ombe, na wakamkabidhi
mtoto kwa Eli. [26] Akasema, “Ee bwana wangu! Kama uishivyo, bwana wangu,
Mimi ndiye yule mwanamke niliyesimama hapa karibu nawe nikimwomba BWANA.
[27] Niliomba kwa ajili ya mtoto huyu na BWANA akawa amenijibu ombi la dua yangu
nililomwomba. [28] Nami nimemtoa kwa BWANA; kwa maisha yake yote, nimempa
BWANA.” Ndipo Elikana na familia yake wakamtukuza BWANA huko Shilo.

# 2

[1] Hana aliomba akasema, “moyo wangu wamtukuza BWANA. Pembe yangu
imejulikana katika BWANA. Kinywa changu kinatamba dhidi ya maadui zangu, kwa
kuwa naufurahia wokovu wako. [2] Hakuna aliye mtakatifu kama BWANA, kwa kuwa
hakuna mwingine zaidi yako; hakuna mwamba kama Mungu wetu. [3] Msijivune sana
hivyo kwa kiburi; vinywa vyenu visitoke majivuno. Kwa kuwa BWANA ni Mungu wa
maarifa; yeye huyapima matendo kwa mizani. [4] Pinde za mashujaa zimevunjika, bali
wale wanaojikwaa hujivika nguvu kama mshipi. [5] Wale walio na shibe ya kutosha
wamejikodisha ili wapate chakula; wale waliokuwa na njaa hawana njaa tena. Hata
yule aliye kuwa tasa amezaa watoto saba, bali mwanamke mwenye watoto wengi
amenyong'onyea. [6] BWANA huua na huuisha. Hushusha kuzimu na huleta tena juu.
[7] BWANA humfanya maskini, na yeye ndiye humtajirisha mtu. Yeye hudhili, lakini
pia hukweza [8] Yeye humwinua juu maskini toka mavumbini: Huwainua wahitaji
toka jalalani na kuwaketisha pamoja na wakuu na kuwarithisha kiti cha enzi cha
utukufu. Kwa kuwa nguzo za dunia ni za BWANA na ameukalisha ulimwengu juu
yake. [9] Yeye atazilinda nyayo za watu wake waaminifu, bali waovu watanyamazishwa
gizani, kwa maana hakuna atayeshinda kwa nguvu zake. [10] Wale wampingao
BWANA watavunjwa vipande vipande; atawapiga radi kutokea mbinguni. BWANA
atahukumu miisho ya dunia; atampa nguvu mfalme wake na kuinua pembe ya
mtiwa mafuta wake.” [11] Nndipo Elikana akenda Rama, nyumbani kwake. Na
yule mtoto akamtumikia BWANA machoni pa Eli, kuhani. [12] Basi, watoto wa Eli
walikuwa wakorofi. Wao hawakumheshimu BWANA. [13] Desturi ya makuhani na watu
ilikuwa kwamba endapo mtu yeyote ametoa dhabihu, mtumishi wa kuhani angekuja
akiwa na uma wa meno matatu mkononi mwake, nyama ilipokuwa inatokoswa.
[14] Naye angeutia uma huo sufuriani, au birikani au chomboni au chunguni; nyama
yote ambayo ingeinuliwa na uma huo ingetwaliwa na kuhani mwenyewe. Ndivyo
walivyofanya huko Shilo kwa Waisraeli wote waliokwenda huko. [15] Tena, kabla ya
kuteketeza mafuta, mtumishi wa kuhani alikuja, na kumwambia aliyekuwa akitoa
dhabihu, “ Tenga nyama ya kuchoma kwa ajili ya kuhani; kwa sababu hataikubali ile
ya kutokosa kutoka kwako, bali tu ile mbichi.” [16] Ikiwa mtu atamwambia, “Wachome
mafuta kwanza, na kisha uchukue kiasi utakacho.” Ndipo angesema, “Hapana,
utanipatia sasa hivi; la sivyo; Nitaichukua kwa lazima.” [17] Dhambi ya vijana hawa
ilikuwa mbaya sana mbele za BWANA, kwa sababu waliidharau dhabihu ya BWANA.
[18] Lakini Samweli alimtumikia BWANA akiwa mdogo akivaa nguo ya naivera ya
kitani. [19] Kila mwaka mama yake alimtengenezea kanzu dogo na kumletea, wakati
wakija na mmewe kutoa dhabihu ya kila mwaka. [20] Eli aliwabariki Elikana na
mke wake na kusema, “BWANA akupatie watoto zaidi kwa mwanamke huyu kwa
sababu ya ahadi yake aliyoitoa kwa BWANA.” Baadaye walirudi nyumbani kwao.
[21] BWANA alimsaidia tena Hana, akawa amebeba mimba nyingine. Akazaa watoto
watatu wa kiume na wa kike wawili. Wakati huo huo mtoto Samweli akakua akiwa
mbele za BWANA. [22] Basi Eli alikuwa mzee sana, akayasikia yote ambayo watoto
wake walikuwa wakiwafanyia Waisraeli wote, na jinsi walivyotembea na mwanamke

aliyekuwa akitumika katika lango la hema ya kukutania. 23 Akawaambia, “Kwa nini
mnafanya mambo hayo? Kwa maana nasikia matendo yenu maovu kutoka kwa watu
hawa wote.” 24 Sivyo hivyo, watoto wangu, maana hii ninayoisikia siyo taarifa njema.
Mnawakosesha watu wa BWANA. 25 “Kama mtu mmoja akimkosea mwenzake, Mungu
atamhukumu; Lakini mtu akimkosea BWANA, ni nani atakayemtetea mtu huyo?”
Lakini hawakuitii sauti ya baba yao, sababu BWANA alinuia kuwaua. 26 Yule mtoto
Samweli aliongezeka umri, na kupata kibali kwa BWANA na kwa watu pia. 27 Kisha
mtu wa Mungu akamwendea Eli na kumwambia, “BWANA asema, 'Je, sikujifunua
mwenyewe kwa nyumba ya baba zako, walipokuwa Misri utumwani nyumbani
mwa Farao? 28 Mimi nilimchagua yeye kutoka makabila yote ya Israeli awe kuhani
wangu, apande madhabahuni kwangu, na kufukiza uvumba, na kuvaa kanzu ya
naivera mbele yangu. Niliwapa nyumba ya baba zako dhabihu zote za wana wa
Israeli zilizotolewa kwa moto. 29 Kwanini basi, unaidharau dhabihu yangu na sadaka
ambazo ninazitaka mahali ninapoishi? Kwanini unawaheshimu watoto wako kuliko
mimi, kwa kujinenepesha ninyi wenyewe kwa uzuri wa kila sadaka ya watu wangu
Israeli?' 30 Maana, BWANA, Mungu wa Isareli, asema, niliahidi kwamba nyumba yako,
na nyumba ya baba yako, yawapasa kwenda mbele zangu milele,' Lakini sasa BWANA
asema. 'Mambo haya yapishe mbali. nami nisifanye hivi, maana nitawaheshimu
wanaoniheshimu, bali wanaonidharau mimi hawatakuwa na thamani. 31 Tazama,
siku zinakuja nitakapoondoa nguvu zako na nguvu za nyumba za baba yako, ili
kwamba pasije kuwepo mtu mzee katika nyumba yako. 32 Nawe utalitazama
hangaiko katika makao yangu. Ingawa Israeli watapewa jambo jema, hapatakuwapo
tena mtu yeyote mzee katika nyumba yako. 33 Yeyote miongoni mwenu nisiye
mwondoa kutoka madhabahuni pangu, Nitasababisha macho yenu yaanguke, na
ita nitasababisha huzuni maishani mwenu. Wanaume wote waliozaliwa katika
familia yako watakufa. 34 Hii ndiyo itakuwa ishara kwako ambayo itawaijia watoto
wako wakiume wawili, juu ya Hofni na Finehasi: Wote wawili watakufa siku moja.
35 Nami nitamwinua juu kuhani wangu mwaminifu atakaye fanya kile kilichomo
moyoni mwangu na nafisini mwangu. Nami nitamjengea nyumba madhubuti; naye
atakwenda mbele ya mfalme wangu mbarikiwa milele. 36 Kila mmoja aliyebakia
nyumbani mwako atakuja na kusujudu mbele ya mtu huyo, akiomba kipande cha
fedha na mkate mmoja, naye atasema, “Tafadhali uniajiri katika moja ya nafasi za
kuhani ili niweze kula kipande cha mkate'”'

# 3

4 1 Yule mtoto Samweli alimtumikia BWANA chini ya uangalizi wa Eli. Neno la
BWANA halikupatikana kwa wingi siku hizo; hapakuwa na maono ya mara kwa
mara ya kinabii. 2 Wakati huo, nguvu ya macho ya Eli ilikuwa imefifia kiasi cha
kutoweza kuona vizuri, na alikuwa amelala kitandani mwake. 3 Ile taa ya BWANA
bado ilikuwa bado inawaka, na Samweli alikuwa amelala katika nyumba ya BWANA,
palipokuwa na sanduku la Mungu. 4 BWANA akamwita Samweli, naye akaitika,
“Niko hapa” 5 Samweli alimwedea Eli na kusema, “Niko hapa, sababu uliniita.” Eli
akasema, “Sikukuita; kalale tena.” Hivyo Samweli akarudi na kulala. 6 BWANA
akamwita tena, “Samweli.” Saamweli aliamka tena na kwenda kwa Eli na kusema,
Niko hapa, sababu umeniita.” Eli akajibu, “Sijakuita, mwanangu; kalale tu tena.”
8 7 Basi Samweli bado hakuwa na uzoefu kuhusu Bwana, wala hakuwahi kupata
ujumbe wowote kutoka kwa BWANA ukifunuliwa kwake. 8 BWANA akamwita tena
Samweli kwa mara ya tatu. Samweli alinyanyuka tena na kwenda kwa Eli na kusema,
“Niko hapa, sababu uliniita,” Ndipo Eli alitambua kwamba BWANA alimwita kijana.
9 Kisha Eli aka, mwambia Samweli, “Nenda ukalale tena; ikiwa atakuita tena, sharti

useme, 'Sema, BWANA, maana mtumwa wako anasikiliza."' Hivyo Samweli akaenda
na kulala mahali pake tena. 10 BWANA alikuja na kusimama; akaita vilevile kama
vile mwanzoni, "Samweli, Samweli." Ndipo Samweli akasema, "Nena, kwa sababu
mtumwa wako anasikiliza." 11 BWANA akasema na Samweli, "Tazama, Niko tayari
kufanya jambo katika Israeli ambalo masikio ya kila mmoja akisikia atashtuka. -
14 12 Siku hiyo nitatimiza kila kitu nilichokisema dhidi ya Eli kuhusu nyumba yake,
kutoka mwanzo hadi mwisho. 13 Nimemwambia kwamba niko tayari kuhukumu
nyumba yake mara moja kwa ile dhambi aliyoifahamu, kwa sababu watoto wake
walijiletea laana juu yao wenyewe na hakuwazuia. 14 Hii ndiyo sababu nimeapa kwa
nyumba ya Eli, kwamba dhambi za nyumba yake hazitasahehewa kwa dhabihu au
kwa sadaka kamwe." 16 15 Samweli akalala hadi asubuhi; baadaye alifungua milango
ya nyumba ya BWANA. Lakini Samweli aliogopa kumwambia Eli kuhusu maono
hayo. 16 Kisha Eli akamwita Samweli na kusema, "Samweli, mwanangu." Samweli
akasema, "Niko hapa." 18 17 Akamuuliza, "Ni neno gani alilokusemesha? Tafadhali
usinifiche jambo hilo. Mungu akutendee hivyo na kukuzidishia, endapo utanificha
kitu chochote kati ya yote ambayo amesema nawe." 18 Samweli akamweleza kila kitu;
hakumficha jambo lolote. Eli akasema, "Ni BWANA. Na afanye linaloonekana jema
kwake." 19 Samweli akakua, na BWANA alikuwa pamoja naye na hakuacha kutimiza
maneno yake ya unabii. 20 Israeli yote tokea Dani hadi Beersheba walijua kwamba
Samweli aliteuliwa kuwa nabii wa BWANA. 21 Naye BWANA alionekana tena huko
Shilo, maana alijifunua mwenyewe kwa Samweli huko Shilo kwa neno lake.

# 4

1 Neno la Samweli likawafikia Israeli wote. Basi Israeli wakatoka kupigana dhidi
ya Wafilisti. Nao wakaweka kambi hapo Ebenezeri, na Wafilisti waliweka kambi
yao huko Afeki. 2 Nao Wafilisti walijipanga kwa ajili ya vita dhidi ya Waisraeli.
Vita ilipopamba moto, Israeli ilishindwa na Wafilisti, wakauawa watu wapatao
elfu nne kwenye uwanja wa vita. 3 Watu walipokuja kambini, wazee wa Israeli
walisema, "Kwa nini BWANA ametushinda leo mbele ya Wafilisti? Hebu tulilete
hapa sanduku la ushuhuda wa BWANA kutoka Shilo, ili kwamba liwe hapa pamoja
nasi, ili litufanye tuwe salama kutokana na nguvu za maadui zetu." 4 Hivyo
waliwatuma watu huko Shilo; kutokea huko walilibeba sanduku la ushuhuda wa
BWANA wa majeshi, akaaye juu ya makerubi. Hofni na Finehasi, watoto wawili
wa Eli, walikuwapo pamoja na lile sanduku la ushuhuda wa Mungu. 5 Sanduku
la ushuhuda wa BWANA lilipofika kambini, watu wote wa Israeli walipiga yowe,
na nchi ikavuma. 6 Wafilisti waliposikia kelele za mayowe, wakasema, "sauti hii
ya mayowe katika kambi ya Waebrania inamaanisha nini?" Baadaye walitambua
kwamba sanduku la BWANA limefika kambini. 7 Wafilisti waliogopa sana, "Mungu
ameingia kambini." Wakasema, "Ole wetu! Jambo kama hili halijawahi kutokea huko
nyuma! 8 Ole wetu! Ni nani atatulinda dhidi ya nguvu za Mungu mwenye uwezo?
Huyu ndiye Mungu aliyewashambulia Wamisri kwa aina tofauti za mapigo mengi
jangwani. 9 Enyi Wafilisti, iweni hodari, na fanyeni kiume, vinginevyo mtakuwa
watumwa wa Waebrabia, kama walivyokuwa watumwa wenu. Fanyeni kiume,
na piganeni nao." 10 Wafilisti walipigana, na Waisraeli wakashindwa. Kila mtu
alikimbilia nyumbani kwake, na mauaji yalikuwa makubwa sana; maana askari wa
Israeli elfu thelathini waendao kwa miguu vitani, walianguka. 11 Lile sanduku la
Mungu lilichukuliwa, na watoto wa Eli, Hofni na Finehasi waliuawa. 12 Mtu mmoja
wa Benjamini alikimbia kutoka uwanja wa vita akaja Shilo siku iyo hiyo, aliwasili na
mavazi yake yamechanika na matope kichwani pake. 13 Alipofika, Eli alikuwa amekaa
kitini pake karibu na barabara akitazama kwa sababu moyo wake ulitetemeka kwa

ajili ya sanduku la Mungu. Mtu yule alipoingia mjini na kutoa taarifa, mji wote ulilia.
[14] Eli aliposikia kelele ya kilio kile, alisema, “Kilio hicho kina maana gani?” Kwa
haraka mtu yule alikuja na kumweleza Eli. [15] Basi Eli alikuwa na umri wa miaka tisini
na nane; macho yake yamepofuka, na hakuweza kuona. [16] Yule mtu akamwambia
Eli, “Mimi ndiye nimechomoka kutoka vitani. Nimetoroka kutoka kwenye mapigano
leo.” Eli akasema, “Mambo yalienda namna gani, mwanangu?” [17] Yule mtu aliyeleta
hizo habari alijibu na kusema, “Israeli wamewakimbia Wafilisti. Pia watu wengi
wameuwawa. Watoto wako, Hofni na Finehasi, wamekufa, na sanduku la Mungu
limechukuliwa.” . [18] Alipotamka sanduku la Mungu, Eli alianguka chali kutoka
kwenye kiti chake karibu na mlango. akavunjika shingo lake, na kufariki, kwa sababu
alikuwa mzee tena mzito. Naye alikuwa mwamuzi wa Israeli kwa miaka arobaini.
[19] Basi mkwewe, mke wa Finihasi, alikuwa mjamzito akikaribia kujifungua. aliposikia
habari kwamba sanduku la Mungu limetekwa nyara na kwamba baba mkwe na mme
wake wamefariki, alichuchumaa chini akajifungua, lakini utungu wake ulimzidi na
ulimtaabisha sana. [20] Alipokaribia kufariki, wanawake waliokuwa wakimhudumia
walisema, “Usiogope, maana umejifungua mtoto wa kiume.” Lakini hakuwajibu
lolote au kuzingatia alichoambiwa. [21] Akamwita mtoto Ikabodi, akisema, “Utukufu
umetoweka Israeli!” Kwa sababu sanduku la Mungu limetekwa nyara, na kwa sababu
ya kifo cha baba mkwe na mme wake. [22] Na alisema, “Utukufu umetoweka kutoka
Israeli, kwa sababu sanduku la Mungu limetekwa nyala.”

# 5

1 Sammweli 5: 1-3 [1] Basi Wafilisti wakawa wamelitwaa sanduku la Mungu,
wakalileta kutoka Ebenezeri hadi Ashdodi. [2] Wafilisti walilichukua sanduku la
Mungu, wakalileta ndani ya nyumba ya Dagoni, na wakalikalisha pembeni mwa
Dagoni. [3] Watu wa Ashdodi walipoamka mapema siku ya pili, tazama, Dagoni
ilianguka chini kifudifudi mbele ya sanduku la BWANA. Hivyo waliichukua Dagoni na
kuisimamisha tena katika sehemu yake.. [4] Lakini walipoamka mapema kesho yake,
tazama, Dagoni alikuwa ameanguka chini kifudifudi mbele ya sanduku la BWANA.
Kichwa cha Dagoni na vitanga vyake miwili vilikatika na kulala mlangoni. Kiwiliwili
cha Dagoni ndicho kilibaki tu. [5] Na hii ndiyo sababu, makuhani wa Dagoni na
yeyote aingiae ndani ya nyumba ya Dagoni, hata leo, hawezi kukanyaga mlango wa
Dagoni katika Ashdodi. [6] Mkono wa BWANA ulikuwa mzito juu ya watu wa Ashdodi.
Aliwaangamiza akawatesa kwa majipu, Ashdodi na wilaya zake kwa pamoja. [7] Watu
wa Ashdodi walipotambua kilichokuwa kinatokea, walisema, “Sanduku la Mungu
wa Israeli lisikae kwetu, kwa sababu mkono wake ni mzito juu yetu na juu ya
mungu wetu Dagoni.” [8] Basi wakawatuma watu wawakusanye pamoja viongozi
wote wa Wafilisti; wakawambia, “Tufanye nini na sanduku la Mungu wa Israeli?”
Wakawajibu, “Sanduku la Mungu wa Israeli lihamishwe na kupelekwa Gathi.” Basi
wakalihamisha hilo sanduku la Mungu wa Israeli hadi huko Gathi. [9] Lakini baada
ya kulipeleka huko, mkono wa BWANA ulikuwa juu ya mji huo, ukasababisha
machafuko makubwa. Akawatesa watu wa mji huo, wakubwa kwa wadogo; na
majipu yakaota juu ya miili yao. [10] Basi, wakalipeleka sanduku la Mungu hadi
Ekroni. Lakini mara tu sanduku la Mungu lilipoingia Ekroni, watu wa Ekroni walipiga
kelele wakisema, “Wametuletea sanduku la Mungu wa Israeli kutuua sisi na watu
wetu.” [11] Basi wakawatuma watu wawakusanye pamoja viongozi wote wa Wafilisti;
wakawambia, “Lipelekeni mbali sanduku la Mungu wa Israeli, na lirudishwe katika
makao yake, ili lisije kutuua sisi na watu wetu.” Kwa maana kulikuwa na hofu ya
kutisha mjini mwote; Mkono wa Mungu ulikuwa mzito mno huko. [12] Watu ambao
hawakufa waliteswa na majipu, na kilio cha mji kilipanda hadi mbinguni.

# 6

[1] Basi sanduku la BWANA lilikaa katika nchi ya Wafilisti kwa miezi saba. [2] Ndipo
Wafilisti wakawaita makuhani na waganga; wakawaambia, “Tulifanyie nini sanduku
la BWANA? Twambieni jinsi ambavyo tunapaswa kulirudisha sanduku katika nchi
yake.” [3] Makuhani na waganga wakasema, “Kama mtalirudisha sanduku la Mungu
wa Israeli, msilipeleke bila zawadi; kwa namna yoyote ile mpelekeeni sadakaa
ya hatia. Hapo ndipo mtapona, na mtajua ni kwanini mkono wake hadi sasa
haujaondoka juu yenu.” [4] Ndipo wakawauliza, “Sadaka ya hatia itakuwa nini
kwamba tunampelekea?” Wakawajibu, “Majipu matano ya dhahabu na panya
watano wa dhahabu, Idadi hiyo ya watano ni sawa na idadi ya viongozi wa Wafilisti.
Kwa sababu tauni ya aina moja iliwashambulia ninyi na viongozi wenu. [5] Kwa
hiyo, nilazima mtengeneze mifano ya majipu yenu, na mifano ya panya wenu
ambayo huiharibu nchi, na mpeni utukufu Mungu wa Israeli. Labda ataondoa
mkono wake kutoka juu yenu, kutoka juu ya miungu yenu, na kutoka juu ya nchi
yenu. [6] Kwanini mfanye mioyo yenu kwa migumu, kama vile Wamisri na Farao
walifanya mioyo yao kuwa migumu? Hicho ni kipindi ambacho Mungu wa Israeli
aliwashughilikia sana; Je, Wamisri hawakuwaachilia watu, na wakaondoka? [7] Basi
sasa, andaeni mkokoteni mpya pamoja na ng'ombe wawili wake wanaonyonyesha,
ambao hawajawahi kufungwa nira. Wafungeni ng'ombe hao kwenye mkokoteni,
lakini warudisheni wale ndama wao nyumbani. [8] Kisha lichukueni sanduku la
BWANA na kuliweka ndani ya mkokoteni. Wekeni ndani ya kasha yale maumbo ya
dhahabu mnayompelekea ambyo ni sadaka ya hatia kando yake. Ndipo mlipeleke
lipate kuondoka. [9] Kisha muwe makini; kama litapanda kwenda kwa njia hadi
nchini mwake hadi Beth Shemeshi, basi mjue kuwa BWANA ndiye aliyetenda pigo
hili kubwa. Lakini kama halitakwenda, ndipo tutajua kwamba siyo mkono wake
uliotupatia mateso; badala yake tutajua kuwa yaliyotupata ilikuwa ni kwa bahati
mbaya tu. [10] Watu hao wakafanya kama walivyoambiwa, walichukuwa ng'ombe
wawili wanaonyonyesha, wakawafunga kwenye mkokoteni, na kuwabakiza ndama
wao nyumbani. [11] Wakaliweka sanduku la BWANA juu ya mkokoteni, pamoja na
lile kasha lililobeba panya wa dhahabu na yale maumbo ya majipu yao. [12] Hao
ng'ombe waliondoka moja kwa moja kuelekea Beth Shemeshi. Walikwenda kwa
kuifuata nija moja kuu, wakiteremka walipokuwa wakienda, na hwakugeuka upande
wa kushoto au kulia. Viongozi wa Wafilisti walifuata kwa nyuma hadi mpaka wa Beth
Shemeshi. [13] Nao watu wa Beth Shemeshi walikuwa wakivuna ngano yao katika
bonde. Waliponyanyua macho yao juu na kuliona sanduku, wakafurahi. [14] Huo
mkokoteni ulifikia ndani ya shamba la Yoshua wa Beth Shemeshi na ukasimama hapo.
Kulikuapo jiwe kubwa mahali hapo, wakatayarisha kuni kutokana na mkokoteni
huo, na wakawatoa ng'ombe hao kama sadaka ya kuteketezwa kwa ajili ya BWANA.
[15] Walawi walilitelemsha sanduku la BWANA chini pamoja na kasha lake lililoyatunza
yale maumbo ya dhahabu, wakaweka vitu hivyo juu ya hilo jiwe kubwa. Watu wa
Beth Shemeshi walitoa sadaka za kuteketezwa na kutoa dhabihu kwa BWANA siku iyo
hiyo. [16] Hao viongozi watano wa Wafilisti walipoona hayo, walirejea Ekroni siku iyo
hiyo. [17] Haya ndiyo majipu ya dhahabu ambayo Wafilisti walirudisha kama sadaka ya
hatia kwa BWANA: moja kwa ajili ya Ashdodi, moja kwa Gaza, moja kwa Ashkeloni,
moja kwa Gathi, na moja kwa Ekroni. [18] Idadi ya wale panya wa dhahabu ilikuwa
sawa na ile ya idadi ya miji yote ya Wafilisti inayomilikiwa na viongozi watano, kwa
miji iliyojengewa maboma na vijiji vya mashambani. Lile jiwe kubwa, ambalo kando
yake waliweka sanduku la BWANA, lipo kama ushuhuda hadi leo katika shamba
la Yoshua Mbeth- Shemeshi. [19] BWANA akawashambulia baadhi ya watu wa Bethi
Shemeshi kwa sababu walichungulia ndani ya sanduku lake. Aliwaua watu sabini.

Watu wakaomboleza, kwa sababu BWANA aliwapa watu pigo kubwa mno. [20] Watu
wa Bethi Shemeshi wakasema, "Ni nani mwenye uwezo wa kushindana na BWANA,
huyu Mungu mtakatifu? Na atampandia nani akitoka kwetu."" Je, ni nani awezaye
kusimama mbele ya BWANA, huyu Mungu mtakatifu? Na ni kwa nani ambako
sanduku litaenda likitoka hapa." [21] Wakawatuma wajumbe kwenda kwa wenyeji wa
Kiriath Yearimu, wakisema, "Wafilisti wamelirudisha sanduku la BWANA; teremkeni
na mkalipeleke kwenu."

# 7

[1] Watu wa Kiriath Yearimu walikuja, wakalichukua sanduku la BWANA, wakalileta
ndani ya nyumba ya Abinadabu mlimani iliyokuwa kilimani. Wakamteua Eleazari,
mwanawe, kulitunza sanduku la BWANA. [2] Tangu siku ambayo sanduku lilikaa
huko Kiiriath Yearimu, ulipita muda mrefu, miaka ishirini. Nyumba yote ya Israeli
iliomboleza na ikaazimu kumrudia BWANA. [3] Samweli akawaambia watu wote wa
Israeli, "Kama mtamrudia BWANA kwa moyo wenu wote, mkaiondoa miungu migeni
na Ashtorethi kutoka katikati yenu, igeuzeni mioyo yenu kwa BWANA, na mwabuduni
yeye peke yake, ndipo atawaokoa kutoka mkono wa Wafilisti." [4] Ndipo watu wa
Israeli wakamuondoa Baali na Ashtorethi, na wakamwabudu BWANA peke yake.
[5] Ndipo Samweli akasema, "Waleteni Israeli wote hadi Mizpa, nami nitamwomba
BWANA kwa ajili yenu." [6] Wakakusanyika Mispa, wakateka maji na kuyamwaga
chini mbele za BWANA. Siku hiyo walifunga na kusema, "Tumemfanyia BWANA
dhambi." Hapo Mispa ndipo Samweli aliwaamu na kuwaongoza watu wa Iraeli. -8
[7] Basi Wafilisti waliposikiakwamba Waisraeli wamekusanyika hapo Mispa, viongozi
wa Wafilisti waliwashambulia Israeli. Waisraeli waliposikia hivyo, waliwaogopa
Wafilisti. [8] Ndipo Waisraeli wakamwambia Samweli, "Usiache kumwomba BWANA
Mungu wetu kwa ajili yetu, ili atuokoe kutoka mkono wa Wafilisti." [9] Samweli
alimchukua kondoo mchanga nakumtoa sadaka ya kuteketezwa kikamilifu kwa
BWANA. Ndipo Samweli akamlilia BWANA kwa ajili ya Israeli, na BWANA akamjibu.
[10] Hata Samweli alipokuwa akitoa sadaka ya kuteketezwa, Wafilisti wakasogea karibu
kuwashambulia Israeli; lakini BWANA alipiga kwa nguromo ya sauti kubwa siku hiyo
dhidi ya Wafilisti na kuwatia kiwewe, na wakashindwa mbele ya Israeli. [11] Waisraeli
wakaondoka Mispa, wakawafuatia Wafilisti na kuwaua hadi kufika chini ya Beth
kari. [12] KIsha Samweli akachukua jiwe akalisimamisha kati ya Mispa na Sheni.
Akaliita hilo jiwe Ebeneza, akisema, "Hata sasa BWANA ametusaidia." [13] Kwa hiyo,
Wafilisti walishindwa na hawakuingia katika mipaka ya Israeli. Mkono wa BWANA
uliwalemea Wafilisti siku zote za Samweli. [14] Miji ambayo Wafilisti waliitwaa kutoka
kwa Israeli ilirudishwa, kutokea Ekroni hadi Gathi; Israeli ikarudisha tena sehemu
za nchi zake kutoka kwa Wafilisti. Ndipo ikawa amani kati ya Israeli na Waamori.
[15] Samweli akawa mwamuzi wa Israeli siku zote za maisha yake. [16] Kila mwaka
aliienda Betheli kwa kuzunguka, akienda Gilgali, na huko Mispa. [17] Kisha angerudi
Rama, kwa sababu mji wake ulikuwa huko; na huko pia aliwaamua Waisiraeli. Hata
huko Rama, pia alimjengea BWANA madhabahu.

# 8

[1] Samweli alipozeeka, aliwaweka watoto wake wawe waamuzi juu ya Israeli.
[2] Mtoto wake wa kwanza aliitwa Yoeli, na mtoto wake wa pili aliitwa Abiya. Hawa
walikuwa waamuzi katika Bersheba. [3] Watoto wake hawakuenenda katika njia za
baba yao, bali walipiga mbio kutafuta mapato ya udhalimu. Walipokea rushwa
na na kupotosha hukumu. [4] Ndipo wazee wote wa Israeli walikutana pamoja na
kumwendea Samweli huko Rama. [5] Wakamwambia, "Angalia, wewe umekuwa mzee,

na watoto wako hawaenendi katika njia zako. Tuchagulie mfalme wakutuamua
kama yalivyo mataifa yote.” 6 Lakini haikumpendeza Sameli waliposema, “Utupatie
mfalme wa kutuamua.” Hivyo akamwomba BWANA. 7 Na BWANA akamwambia
Samweli, “Sikiliza sauti ya watu kwa kila jambo wanalokwambia; kwa sababu
hwajakukataa wewe, bali wamenikataa mimi nisiwe mfalme wao. 8 Sasa wanafanya
kama vile walivyotenda tangu siku ile nilipowatoa huko Misri, kwa kuniacha,
na kuwatumikia miungu mingine, na ndivyo hivyo pia wanakufanyia na wewe.
9 Basi sasa uwasikilize; lakini uwaonye sawasawa na uwafahamishe tabia ya
mfalme atakaye waongoza. 10 Kwa hiyo Samweli akawaambia watu waliokuwa
wakiomba mfalme maneno yote ya BWANA. 11 Akasema, “Hivi ndivyo jinsi mfalme
atakavyowatawala. 12 Atawachukua watoto wenu wa kiume na kuwaweka juu ya
magari ya vita na kuwa wapanda farasi wake, na kukimbia mbele ya magari yake.
Atawaweka ma- kapteni wake juu ya maelfu ya askari, na ma-kapteni juu ya askari
hamsini. Wengine atawafanya wakulima wamashamba yake, wengine wavunaji wa
mazao yake, wengine watatengeneza silaha zake na zana za magari yake. 13 Naye
atawachukua binti zenu kuwa watengeneza manukato, wapishi, na waoka mikate.
14 Atachukua mashamba yenu mazuri, mashamba ya mizabibu, na yale ya mizeituni
na kuwapa watumishi wake. 15 Atachukua moja ya kumi ya nafaka zenu na mizabibu
na na kuwapa maofisa na watumishi wake. 16 Atawachukua watumwa wenu na
wajakazi wenu na vijana wenu waliowazuri na punda wenu; atawatumikisha wote
kwa ajili yake. 17 Atawatoza moja ya kumi ya mifugo yenu, na mtakuwa watumwa
wake. 18 Ndipo mtalia siku ile kwa sababu ya mfalme wenu mliyemchagua kwa
ajili yenu; lakini siku ile BWANA hatawajibu 19 Lakini watu walikataa kumsikiliza
Samweli; wakasema, “Hapana!” Lazima awepo mfalme juu yetu. 20 Ili tuweze kuwa
kama mataifa mengine yote, na hivyo mfalme wetu aweze kutuamua na atoke mbele
yetu na atupiganie vita yetu. 21 Naye Samweli aliposikia maneno yote ya watu,
akayarudia katika masiko ya BWANA. 22 BWANA akamwambia Samweli, “Sikiliza
sauti yao na uwafanyie mfalme.” Hivyo Samweli akawaambia watu wa Israeli, “Kila
mtu na arudi mjini kwake.”

# 9

Samweli 9: 1-2 1 Basi kulikuwa na mtu mmoja kutoka Benyamini, mtu mashuhuri.
Jina lake aliitwa Kishi mwana wa Abieli, mwana wa Zerori, mwana wa Bekorathi,
mwana wa Afia, mwana wa Mbenyamini. 2 Huyu alikuwa na mtoto wa kiume
aliyeitwa Sauli, kijana mzuri wa uso. Hapakuwapo mwanaume mzuri wa uso kuliko
huyu miongoni mwa watu wote wa Israeli. Kutoka mabegani kwenda juu alikuwa
mrefu kuliko watu wengine. 3 Na punda wa Kishi, baba yake na Sauli walipotea.
hivyo Kishi akamwambia Sauli mwanawe, “Mchukue mmoja wa watumishi; uamke
uende kuwatafuta punda,” 4 Sauli akapita katika nchi ya vilima vilima ya Efraimu
na akaenda akapita katika nchi ya Shalisha, lakini hawakuwaona. Kisha walipita
katika nchi ya Shaalimu, lakini hawakuwa huko. Baadaye alipita katika nchi ya
Wabenyamini, lakini hawakuwaona wale punda. 5 Na walipofika nchi ya Sufu,
Sauli alimwambia mtumishi wake aliyekuwa naye, “Njoo na turudi, pengine baba
aweza kuacha kuchunga punda na kuanza kutuhofia sisi.” 6 Lakini mtumishi
akamwmbia, “Sikiliza, Yupo mtu wa Mungu katika mji huu. Naye ni mtu wa
kuheshimiwa sana; kila asemalo huwa kweli. Hebu twende huko; labda anaweza
kutuambia tupitie wapi katika safari yetu.” 7 Ndipo Sauli akamwambia mtumish
iwake, “Lakini kama tukienda kwake, twaweza kumpelekea nini? Maana hata mkate
katika mfuko wetu umekwisha, na hakuna zawadi ya kumpelekea mtumishi wa
Mungu. Tuna kitu gani? 8 Huyo mtumishi akamjibu Sauli na kusema, “Hapa,

ninayo robo ya shekeli ya fedha ambayo nitampa mtumishi wa Mungu, atuambie
ni njia ipi yatupasa tuiendee.” 9 (Zamani katika Israeli, mtu alipotaka kujua neno
kuhusu mapenzi ya Mungu, alisema, “Njoo, haya twende kwa mwonaji.” Kwa
maana nabii wa leo, zamani aliitwa Mwonaji). 10 Ndipo Sauli akamwambia mtumishi
wake, “Umesema vyema. Haya, njoo twende.” Basi wakaenda katika mji ambao
mtu wa Mungu alikuwamo. 11 Walipopanda mlima kuelekea mjini, walikutana na
wasichana wakienda kuteka maji; Sauli na mtumishi wake wakawauliza, “Mwonaji
hupo hapa?” 12 Nao wakawajibu, na kusema, “Yupo; tazameni, yuko mbele yenu.
Harakisheni, kwa maana anakuja mjini leo, sababu leo watu wanatoa dhabihu zao
mahali pa juu. 13 Mara tu mtakapoingia mjini mtamuona, kabla hajapanda mahali
pa juu kla chakula. Watu hawatakula hata atakapokuja, kwa sababu ndiye ataibariki
dhabihu; na baadaye wale ambao wamealikwa hula. Basi pandeni, mtamuona sasa
hivi.” 14 Kwa hiyo walikwea kwenda mjini. Walipokuwa wakiingia mjini, walimuona
Samweli akija mbele yao, akipanda kwenda mahali pa juu. 15 Siku moja kabla
Sauli hajafika, BWANA alikuwa amemfunulia Samweli: 16 “Kesho wakati kama huu
nitakutumia mtu kutoka nchi ya Benyamini, nawe utamtia mafuta awe mfalme juu
ya watu wangu Israeli. Atawaokoa watu wangu kutoka mkono wa Wafilisti. Kwa
kuwa nimewaonea huruma watu wangu na kilio cha kutaka msaada kimenifikia.”
17 Samweli alipomuona Sauli, BWANA akamwambia, “Huyu ndiye mtu niliyekwambia
habari zake! Yeye ndiye atakayewatawala watu wangu.” 18 Ndipo Sauli akaja
karibu na Samweli katika lango na kusema, “Niambie nyumba ya Mwonaji iko
wapi? 19 Samweli akamjibu Sauli akisema, “Mimi ndiye mwonaji. Tangulia mbele
hadi mahali pa juu, nami nitakueleza kila kitu kilichomoyoni mwako. 20 Kama
punda wenu waliopotea siku tatu zilizopita, msihofu kuhusu hao punda, kwa kuwa
wamekwishapatikana. Na yote yaliyotamanika kwa ajili ya Israeli yanamwangukia
nani? Siyo kwako na nyumba ya baba yako yote?” 21 Sauli akamjibu na kusema, Siyo
mimi Mbenyamini, kutoka kabila lililo dogo sana kwa makabila ya Israeli? Siyo ukoo
wangu ulio mdogo sana kwa kabila la Benyamini? Kwa nini basi unaniambia kwa
namna hii?” 22 Hivyo Samweli akamchukua Sauli na mtumishi wake, akawaingiza
ukumbini, akawakalisha mahali pa heshima pa wale walioalikwa, idadi yao takribani
watu thelathini. 23 Samweli akamwambia mpishi, “Lete sehemu niliyokupatia,
sehemu ambayo nilikwambia hivi, “Itenge.”' 24 Basi mpishi alichukua paja lililokuwa
limeinuliwa katika dhabihu na kile kilichokuwa pamoja nalo, akaitenga mbele ya
Sauli. Kisha Samweli akasema, “Angalia kile kilichokuwa kimetunzwa kwa ajili
yako! Kula, kwa sababu kilitunzwa hadi wakati maalum ufike kwa ajili yako. Na
kwa sasa waweza kusema, 'Nimewaalika watu.”' Kwa hiyo Sauli alikula pamoja na
Samweli siku hiyo. 25 Walipokuwa wamekwisha shuka chini kutoka sehemu ya juu
na kuingia mjini, Samweli akazungumza na Sauli darini. 26 Na kulipopambazuka,
Samweli alimwita Sauli darini na kusema, “Amka, kusudi nikusindikize uende
zako,” Hivyo Sauli aliamka, na wote wawili, yeye na Samweli walitoka kwenda
mtaani. 27 Walipokuwa wakienda nje ya viunga vya mji, Samweli akamwambia Sauli,
“Mwambie mtumishi wako atanguliye mbele yetu(na alitangulia mbele), Lakini wewe
sharti usubiri kidogo, nipate kukuambia ujumbe wa Mungu.”

## 10

1 Ndipo Samweli akachukua chupa ya mafuta, akayamimina juu ya kichwa cha
Sauli, na akambusu. Akasema, “Je, Mungu hajakutia mafuta uwe mtawala juu ya
urithi wake? 2 Utakapoondoka kwangu leo, utawaona wanaume wawili na kaburi
la Raheli, katika nchi ya Benyamini hapo Selsa. Watu hao watakuambia, 'Wale
punda mliokuwa mkiwatafuta wamepatikana. Sasa, Baba yako ameacha kuwatunza

punda, na ana hofu juu yenu, anasema, “Nitafanya nini kuhusu mwanangu?” 3 Kisha
utakwenda mbele kutoka hapo, na utafika katika mwaloni wa Tabori. Utakutana
na watu watatu hapo wakienda kwa Mungu huko Betheli, mmoja akibeba wana-
mbuzi watatu, mwingine akibeba mikate mitatu, na mwingine akibeba kiriba cha
divai. 4 Watawasalimu na watawapatia mikate miwili, kutoka mikononi mwao.
5 Baada ya hayo, utafika katika mlima wa Mungu, mahali ilipo ngome ya Wafilisti.
Utakapofika mjini, utakutana na kundi la manabii wakiteremka chini kutoka mahali
pa juu wakiwa na kinanda, tari, kinubi na filimbi mbele yao; na watakuwa wakitabiri.
6 Roho ya BWANA itakujaza, nawe utatabiri pamoja nao, na utabadilishwa na kuwa
mtu tofauti. 7 Basi, ishara hizi zikikufikia, fanya lolote ambalo mikono yako itaona
ifanye, kwa sababu Mungu yu pamoja nawe. 8 Nenda ushuke mbele yangu hadi
Gilgali. Kisha nitakufuata huko nitoe dhabihu za kuteketezwa na kutoa dhabihu
za amani. Nisubiri kwa muda wa siku saba hadi nije kwako na nikuoneshe
unachopaswa kufanya.” 9 Sauli alipotega mgongo amuache Samweli, Mungu akampa
moyo mwingine. Ndipo ishara zote hizi zikatimia siku hiyo. 10 Walipofika mlimani,
kundi la manabii lilikutana naye, na Roho ya Mungu ikamjilia kwa nguvu ili
atabiri pamoja nao. 11 Kila mtu aliyemfahamu kabla hajamwona akitabiri pamoja
na manabii, watu waliambizana wao kwa wao,:”Kitu gani kimempata mtoto wa
Kishi? Hivi Sauli ni mmoja wa manabii siku hizi?” 12 Mtu mmoja kutoka eneo
hilo akajibu, “Na ni nani baba yao?” Kwa sababu ya jambo hili, ukawapo msemo,
“Hivi Sauli naye ni mmoja wa manabii?” 13 Alipomaliza kutabiri, akafika mahali
pa juu. 14 Ndipo baba yake mdogo na akamuuliza Sauli na mtumishi wake,
“Mlienda wapi?” Naye akamjibu, “Kuwatafuta punnda; tulipoona kwamba hatuwezi
kuwapata, tukaenda kwa Samweli.” 15 Baba yake mdogo akasema, “Tafadhali
niambie kile alichosema kwako Samweli,” 16 Sauli akamjibu baba yake mdogo,
“Alituambia waziwazi kwamba punda wamepatikana.” Lakini kuhusu swala la
ufalme alilosema Samweli hakumwambia. 17 Basi Samweli aliwaita watu pamoja
huko Mispa. 18 Akwaambia watu wa Israeli, “Hivi ndivyo BWANA, Mungu wa Israeli
asemavyo: 'Niliwatoa Israeli kutoka Misri, na niliwaokoa kutoka nchi ya Wamisri,
na kutoka mkono wa falme zote zilizowaonea.' 19 Lakini leo mmemkataa Mungu
wenu, awaokoaye kutoka kwenye majanga na mahangaiko; na mmemwambia, '
Tuwekee mfalme juu yetu,; Sasa jihudhurisheni wenyewe mbele za BWANA kwa
kabila na jamaa zenu.” 20 Kisha Samweli akawaleta kabila zote za Isareli karibu,
na kulichagua kabila la Benyamini. 21 Akawasogeza karibu kabila la Benyamini kwa
kufuata jamaa zao; na jamaa ya Wamatri ikachaguliwa; na Sauli mwana wa Kishi
akachaguliwa. Lakini walipokwenda kumtafuta, hakuweza kuonekana. 22 Kisha
watu walitaka kumuuliza Mungu maswali zaidi, “Bado yupo mtu mwingine ajaye?”
BWANA akajibu, “ Yeye mwenyewe kajificha kwenye mizigo.” 23 Wakaenda mbio
na kumleta Sauli kutoka humo. Aliposimama kati yao, alikuwa mrefu kuliko watu
wote kuanzia mabega yake kwenda juu. 24 Kisha Samweli akawaambia watu, “Je,
mnamuona mtu ambaye BWANA amemchagua? Hakuna mtu kama yeye kati ya watu
wote.” Watu wote wakapiga Kelele, “Mfalme na aishi” 25 Ndipo Samweli akawaambia
watu desturi na sheria za ufalme, akaziandika katika kitabu, na kuziweke mbele za
BWANA. Baadaye Samweli akawaruhusu watu waondoke kila mtu aende nyumbani
kwake. 26 Sauli pia alienda nyumbani kwake huko Gibea, akiwa na baadhi ya
watu wenye nguvu, wenye mioyo iliyoguswa na Mungu. 27 Lakini baadhi ya watu
wasiofaa walisema, “Huyu mtu atatuokoaje?” Watu hawa walimdharau Sauli na
hawakumletea zawadi zozote. Lakini Sauli alinyamaza kimya.

# 11

1 Ndipo Nahashi Mwamoni akaenda na kupiga kambi kuzunguka Yabeshi Gileadi.
Watu wote wa Yabeshi wakamwambia Nahashi, “Fanya mkataba nasi, na tutaku-
tumikia,” 2 Nahashi Mwamoni akawajibu, “Kwa sharti hili nitafanya mkataba na
ninyi, kwamba wote niwang'oe macho ya kulia, na kwa kitendo hiki kilete fedheha
katika Israeli yote.” 3 Basi wazee wa Yabeshi wakamjibu, “Tuache kwa siku saba,
ili tuwatume wajumbe katika nchi yote ya Israeli. Ndiposa, kama hakuna mtu wa
kutuokoa, tutasalimu amri kwako.” 4 Nao wajumbe wakafika Gibea, alipoishi Sauli,
na wakawaeleza watu kile kilichotokea. Watu wote wakalia kwa sauti kuu. 5 Na
Sauli alikuwa akiwafuata nyuma maksai kutoka shambani. Sauli akauliza, “Watu
wamepatwa na nini hadi wanalia?” Ndipo wakamweleza Sauli kile ambacho watu
wa Yabeshi walikisema. 6 Sauli aliposikia kile walichosema, Roho ya Mungu ikamjia
kwa nguvu, na akakasirika. 7 Akashika nira ya maksai, akawakata hao ng'ombe
vipande vipande, na akavituma hivyo vipande katika nchi yote ya Israeli kwa
kuwatumia wajumbe, Akasema, “Yeyote asiyejitokeza akimfuata Sauli na Samweli,
hivi ndivyo ng'ombe wake watakavyofanywa.” Na hofu ya BWANA ikawaingia
watu, na wakajitokeza wote kwa pamoja. 8 Alipowahesabu hapo Beseki, watu wa
Israeli walikuwa elfu mia tatu, na watu wa Yuda elfu thelathini. 9 Wakawaambia
wale wajumbe waliotumwa, “Mtawaambia watu wa Yabeshi Gileadi, 'Kesho, wakati
wa jua kali, Mtaokolewa.”' Basi wale wajumbe wakaenda na kuwaambia watu
wa Yabeshi, na watu wakafurahi. 10 Ndipo watu wa Yabeshi wakamwambia
Nahashi, “Kesho tutasalimu amri kwako, na utaweza kutufanyia chochote unachoona
kinakupendeza.” 11 Siku iliyofuata Sauli akawapanga watu katika vikosi vitatu.
Wakafika katikati ya Kambi wakati wa asubuhi, wakawashambulia na kuwashinda
Waamoni ilipofika mchana. Waliosalimika nao walitawanyika, kiasi kwamba hata
watu wawili hawakuachwa pamoja. 12 Ndipo watu wakamwambia Samweli, “Wako
wapi waliosema, 'Hivi kweli Sauli atatutawala?' Walete watu hao, ili tuwauwe.”
13 Lakini Sauli akasema, “Hakuna atakayeuwawa siku ya leo, kwa sababu leo BWANA
amemuokoa Isreli.” 14 Kisha Samweli akawaambia watu, “Njoni, twendeni Gilgali na
tuimarishe ufalme tena huko.” 15 Hivyo watu wote wakaenda Gilgali na wakamsimika
Sauli kuwa mfalme mbele za BWANA huko Gilgali. Na huko walitoa sadaka za amani
mbele za BWANA, na watu wote wa Israeli wakafurahi sana.

# 12

1 Samweli aksema na Israeli wote, “Nimesikia kila kitu mlichoniambia, na
nimemweka mfalme juu yenu. 2 Basi, yupo hapa mfalme aliyeko mbele yenu, mimi
nimezeeka nakujaa mvi; na watoto wangu wako pamoja nanyi. Nimekuwa kiongozi
wenu tangu ujana wangu hadi leo. 3 Mimi niko hapa, Nishuhudieni mbele za BWANA
na mbele za mtiwa mafuta wake. Nimechukua ng'ombe wa nani? Nimechukua
punda wa nani? Ni nani nimemdhulumu? Nimemwonea nani? Nimepokea rushwa
kutoka mikono ya nani inipofushe macho yangu? Nishuhudieni, nami nitawarudishia
4 Nao wakasema, Haujatudanganya, kutuonea, au kuiba chochote kutoka mkono wa
mtu yeyote.” 5 Akawaambia, “BWANA ni shahidi juu yenu, na masihi wake leo ni
shahidi, kwamba hamkuona kitu mkononi mwangu.” Na wao wakajibu, “BWANAni
shahidi.” 6 Samweli akawaambia watu, “BWANA ndiye aliyemteua Musa na Haruni,
na ndiye aliyewatoa baba zenu kutoka nchi ya Misri. 7 Basi sasa, jihudhurisheni,
ili niweze kutoa utetezi juu yenu kwa BWANA kuhusu matendo yote ya haki ya
BWANA, ambayo aliwafanyia ninyi na baba zenu. 8 Yakobo alipokuwa amefika Misri,
na babu zenu walimlilia BWANA. BWANA alimtuma Musa na Haruni, waliowaongoza
babu zenu kutoka Misri na wakaja kukaa sehemu hii. 9 Lakini walimsahau BWANA

Mungu wao; akawauza katika mkono wa Sisera, jemedari wa majeshi ya Hazori,
katika mkono wa Wafilisti, na katika mkono wa mfalme wa Moabu; hawa wote
walipigana na babu zenu. 10 Wakamlilia BWANA mkasema, 'Tumefanya dhambi, kwa
sababu tumemwacha BWANA na tumewatumikia Mabaali na Mashtorethi. Lakini
sasa tuokoe kutoka mikono ya maadui zetu, na tutakutumikia.' 11 Hivyo BWANA
akawatuma Yerubu Baali, Bedani, Yefta na Samweli, na akawapa ushindi dhidi ya
maadui zenu wote waliowazunguka, na kwamba mliishi kwa amani. 12 Mlipoona
kwamba Nahashi mfalme wa watu wa Amoni amekuja dhidi yenu, mkaniambia,
'Hapana! Badala yake, mfalme awepo atawale juu yetu'- ingawa BWANA, Mungu
wenu, alikuwa mfalme wenu. 13 Sasa yupo hapa mfalme ambaye mmemchagua,
mliyemuomba na ambaye BWANA amemteua awe mfalme juu yenu. 14 Ikiwa
mnamhofu BWANA, mtumikieni, muitii sauti yake, msikaidi amri ya BWANA, basi
wote wawili ninyi na mfalme anayewatawala mtakuwa wafuasi wa BWANA Mungu
wenu. 15 Kama hamtaitii sauti ya BWANA, mkaasi amri za BWANA, ndipo mkono
wa BWANA utakuwa juu yenu, kama ulivyokuwa juu ya babu zenu. 16 Hata sasa
muwepo kabisa na muone jambo kubwa ambalo BWANA atalifanya mbele ya macho
yenu. 17 Je, leo si mavuno ya ngano? Nitamwomba BWANA, naye ataleta ngurumo
na mvua. Ndipo mtajua na kuona kwamba uovu wenu ni mwingi, mlioufanya
machoni pa BWANA, kujiombea mfalme wenu ninyi wenyewe." 18 Hivyo Samweli
akamwomba BWANA; na siku iyo hiyo BWANA akatuma ngurumo na mvua. Ndipo
watu wote wakamwogopa sana BWANA pamoja na Samweli. 19 Kisha watu wote
wakamwambia Samweli, "Waombee watumishi wako kwa BWANA Mungu wako, ili
tusife. Kwa maana tumeongeza uovu huu juu ya dhambi zetu tulipojiombea mfalme
sisi wenyewe." 20 Samweli akawajibu, "Msiogope. Mmefanya uovu wote huu, lakini
msigeukie mbali na BWANA, bali mtumikieni BWANA kwa moyo wenu wote. 21 Wala
msigeuke na kufuata mambo matupu yasiyo na faida au kuwaokoa, kwa sababu ni
ubatili. 22 Kwa ajili ya jina lake kuu, BWANA hatawakataa watu wake, kwa sababu
imempendeza BWANA kuwafanya ninyi kuwa watu kwa ajili yake. 23 Kwangu mimi,
iwe mbali nami kumtenda BWANA dhambi kwa kuacha kuwaombea ninyi. Badala
yake, nitawafundisha njia iliyo njema na sahihi. 24 Mcheni BWANA tu na mtumikieni
yeye katika kweli kwa moyo wenu wote. Tafakarini mambo makuu aliyowatendeeni.
25 Lakini kama mtadumu kufanya uovu, ninyi wote na mfalme wenu mtaangamizwa."

# 13

1 Sauli alikwa na umri wa miaka [thelathini] alipoanza kutawala; alipokuwa
ametawala Israeli kwa miaka [arobaini], 2 aliwachagua wanaume elfu tatu wa
Israeli. Elfu mbili walikuwa pamoja naye huko Mikmashi na katika nchi ya
milima ya Betheli, wakati huo wale elfu moja walikuwa pamoja na Yonathani
katika Gibea ya Benyamini. Askari waliobaki aliwarudisha nyumbani, kila mtu
hemani kwake. 3 Yonathani akaishinda ngome ya jeshi la Wafilisti iliyokuwa
Geba na Wafilisti wakasikia habari hiyo. Baadaye Sauli alipiga tarumbeta katika
nchi yote, akisema, "Sikieni enyi Waebrania." 4 Israeli yote imesikia kwamba
Sauli ameipiga ngome ya Wafilisti, na pia kwamba Israeli imekuwa uvundo kwa
Wafilisti. Ndipo askari wakaitwa kwa pamoja kuungana na Sauli huko Gilgali.
5 Wafilisti walijikusanya pamoja kupigana dhidi ya Waisraeli: magari elfu tatu,
watu elfu sita wakuendesha magari, na majeshi mengi kama mchanga ufukoni mwa
bahari. Wakapanda na kupiga kambi huko Mikimashi, mashariki mwa Beth aveni.
6 Watu wa Israeli walipoona kuwa wapo katika matatizo -kwa maana watu walikata
tamaa, wakajificha kwenye mapango, kwenye vichaka, kwenye miamba, kwenye
visima na katika mashimo. 7 Baadhi ya Waebrania walipanda kwenda Yordani

katika nchi ya Gadi na Gileadi. Lakini Sauli alibaki Gilgali, na watu waliomfuata
wakitetemeka. [8] Alisubiri kwa siku saba, muda uliopangwa na Samweli. Lakini
Samweli hakufika huko Gilgali, na watu wakatawanyika mbali na Sauli. [9] Sauli
akasema, “Nileteeni sadaka ya kuteketezwa na sdaka ya amani.” Kisha akatoa
sadaka ya kuteketezwa. [10] Mara tu alipomaliza kutoa sadaka ya kuteketezwa Samweli
akawasili. Sauli akatoka nje wakutane na kumsalimia. [11] Basi Samweli akasema,
“Umefanya nini?” Sauli akajibu, “Nilipoona kwamba watu wanaiacha, na kwamba
umechelewa hukufika kwa muda uliopangwa, na kwamba Wafilisti wamekwisha
jikusanya huko Mikmashi, [12] nikasema, 'Sasa Wafilisti watashuka dhidi yangu huko
Gilgali, na sijaomba kibali cha BWANA.' Kwa hiyo nikajilazimisha mwenyewe kutoa
sadaka ya kuteketezwa.” . [13] Ndipo Samweli akamwambia Sauli, “Umetenda mambo
ya kipumbavu. Hukuheshimu amri ya BWANA Mungu wako aliyokupatia. Kwa
maana BWANA angeutengeneza utawala wako juu ya Israeli milele. [14] Lakini sasa
utawala wako hautaendelea. BWANA ametafuta mtu anayekubaliwa na moyo wake,
kwa sababu wewe hukutii alichokuamuru.” [15] Ndipo Samweli akasimama akapanda
kutoka Gilgali hadi Gibea ya Benyamini. Basi Sauli akawahesabu watu waliokuwapo
pamoja naye, idadi yao ilikuwa kama watu mia sita. [16] Sauli, mtoto wake Yonathani,
na watu waliokuwa pamoja nao, wakabaki Geba ya Benyamimni. Lakini Wafilisti
wakapiga kambi huko Mikmashi. [17] Wateka nyara makundi matatu wakaja kutoka
kambi ya Wafilisti. Kundi moja likapinda kuelekea Ofra, hadi nchi ya Shuali. [18] Kundi
jingine likageuka kuelekea Bethholoni, na kundi jingine likaelekea katika mpaka
kulikabili bonde la Seboimu kuelekea jangwani. [19] Hakuna hata mhunzi aliyeonekana
katika nchi yote ya Israeli, kwa sababu Wafilisti walisema, “ Waebrania wasije
wakajitengenezea mapanga au mikuki.” [20] Lakini Waisraeli wote huwa wakiteremka
kwa Wafilisti, kila mtu kunoa jembe lake, sululu yake, shoka lake na mundu wake.
[21] Gharama za kunoa ncha za majembe, sululu, mashoka na kunyoosha michokoo
ilikuwa theluthi moja ya shekeli. [22] Hivyo siku ya vita, hakukuwa na mapanga
au mikuki iliyoonekana katika mikono yoyote ya askali waliokuwa na Sauli na
Yonathani; Ni Sauli na mtoto wake tu ndio walikuwa nazo. [23] Vikosi vya Wafilisti
wakatokeza katika nija ya Mikmashi.

# 14

[1] Siku moja, Yonathani mwana wa Sauli alimwambia mbeba silaha wake aliye
mdogo, “Njoo, hebu twende hadi upande mwingine kwenye ngome ya Wafilisti.”
Lakini hakumjulisha baba yake. [2] Sauli alikuwa akikaa nje ya mji wa Gibea chini
ya mti wa mkomamanga ulio katika Migroni. Takribani watu mia sita walikwa
pamoja naye, [3] akiwemo Ahiya mwana wa Ahitubu (nduguye Ikabodi) mwana wa
Finehasi, mwana wa Eli, kuhani wa BWANA huko Shilo, aliyevaa naivera. Watu
hao hawakujua kwamba Yonathani ameondoka. [4] Katikati ya vichochoro, ambavyo
Yonathani alinuia kuvipita hadi ngome ya Wafilisti, kulikuwa na mwamba wenye
mteremko mkali upande mmoja, na mteremko mkali upande mwingine. Jabali moja
liliitwa Bosesi, na jingine liliitwa Sene. [5] Lile jabali lenye mteremko mkali zaidi
liliinuka upande wa kaskazini mbele ya Mikmashi, na jingine upande wa kusini
mbele ya Geba. [6] Yonathani akamwambia kijana mbeba silaha, “Njoo, na tuvuke
hadi ngome ya hawa wasiotahiriwa. Pengine BWANA atatenda kwa niaba yetu, kwa
maana hakuna kitu kiwezacho kumzuia BWANA asiokoe kwa wengi au kwa watu
wachache.” [7] Mbeba silaha wake akajibu, “Fanya kila kitu kilicho ndani ya moyo
wako. Songa mbele, tazama, niko pamoja nawe, nitatii maagizo yako yote.” [8] Ndipo
Yonathani akasema, “Tutavuka twende kwa watu hao, na tutajionesha wenyewe
kwao. [9] Kama watatuambia, 'Subirini hapo hadi tutakapokuja kwenu' - basi tutabaki

katika sehemu yetu na hatutavuka kwenda kwao. 10 Lakini kama watajibu, 'Njoni
kwetu,' ndipo tutavuka; kwa sababu BWANA amewaweka mkononi mwetu. Hii
ndiyo itakuwa ishara yetu.” 11 Kwa hiyo wote wawili wakajifunua mbele ya ngome
ya Wafilisti. Wafilisti wakasema, “Angalia, Webrania wanakuja kutokea kwenye
mashimo walimojificha.” 12 Ndipo watu wa ile ngome wakamwita Yonathani na
mbeba silaha wake, wakisema, “Njoni huku kwetu, tutawaonesha jambo fulani.” Na
Yonathani akamwambia mbeba silaha wake; “Nifuate nyuma yangu, kwa sababu
BWANA amewaweka katika mkono wa Israeli.” 13 Yonathani alipanda juu kwa
mikono na miguu yake, na mbeba silaha akimfuata nyuma yake. Wafilisti waliuwawa
mbele ya Yonathani, na mbeba silaha wake akiwaua baadhi nyuma yake. 14 Hilo
shambulio la kwanza walilofanya Yonathani na mbeba silaha wake, waliua watu
wapatao ishirini katika urefu wa nusu handaki kwenye eka moja ya ardhi. 15 Kukawa
na hofu kubwa katika kambi, uwandani, na katika watu. Hata ngome ya jeshi na
watekaji nyara nao wakawa na hofu kubwa 16 Ndipo walinzi wa Sauli huko Gibea
ya Benyamini wakaona kundi la askari wa Wafilisti likitawanyika, wakienda kule na
huku. 17 Kisha Sauli akawaambia watu aliokuwa nao, “Mjihesabu ili muone nani
hayupo hapa.”Walipokuwa wamehesabu, wakagundua kuwa Yonathani na mbebaji
wa silaha zake hawapo. 18 Sauli akamwambia Ahiya, “Lete hapa naivera ya Mungu”-
kwa maana siku hiyo Ahiya alivaa naivera akiwa pamoja na askari wa Israeli.
19 Wakati Sauli akiongea na kuhani, kelele na ghasia kubwa iliendelea na kuongezeka
katika kambi ya Wafilisti. dipo sauli akamwambia kuhani, “Acha kazi unayofanya.”
20 Sauli na watu wote aliokuwa nao wakajipanga na kwenda kwenye mapigano.
Upanga wa kila Mfilisti ulikwa juu ya Mfilisti mwenzake, na kulikuwa na ghasia
kubwa. 21 Basi Waebrania ambao mwanzoni walijiunga na Wafilisti, na kwenda
kwenye kambi yao, wao pia waliungana na Waisraeli waliokuwa pamoja na Sauli
na Yonathani. 22 Waisraeli wote waliokuwa wamejificha katika milima karibu na
Efraimu waliposikia kwamba Wafilisti wamekimbia, nao pia wakawafuata Wafilisti
nakuwafukuza kwenye hiyo vita. 23 Hivyo siku hiyo BWANA aliwaokoa Israeli, na
mapigano yalivuka kupitiliza Beth aveni. 24 Siku hiyo watu wa Israeli walifadhaika
kwa sababu Sauli aliwaweka watu chini ya kiapo akasema, “Na alaaniwe mtu
atakaye kula chakula kabla ya jioni na kabla sijalipiza kisasi kwa maadui zangu.”
Hivyo hakuna hata mmoja kati ya watu wote aliyeonja chakula. 25 Ndipo watu
wote wakaingia msituni na kuona asali ikiwa juu ya ardhi. 26 Watu walipoingia
humo msituni, asali ilitiririka, lakini hakuna aliyeweka mkono wake kinywani kwa
maana watu waliogopa kiapo. 27 Lakini Yonathani alikuwa hajasikia kwamba baba
yake amewaagiza watu kwa kiapo. Akanyoosha ncha ya fimbo iliyokuwa mkononi
mwake na kuichovya kwenye sega la asali. Kisha akanyoosha mkono wake hadi
kinywani mwake, na macho yake yakaangaziwa. 28 Ndipo mmoja wa watu hao,
akamwambia, “Baba yako aliwaagiza watu kwa mkazo na kwa kiapo, kwa kusema,
'Alaaniwe mtu atakaye kula chakula kwa siku ya leo,' ingawa watu wamedhoofika
kwa ajili ya njaa.” 29 Baadaye Yonathani alisema, “Baba yangu amefanya matatizo
katika nchi. Angalia jinsi macho yangu alivyotiwa nuru kwa sababu nilionja asali
hii kidogo. 30 Je, siyo vivuri sana kama leo watu wangekula bila kizuizi nyara
walizopata kutoka kwa maadui zao? Kwa sababu sasa mauaji hayakuwa makubwa
katikati ya Wafilisti.” 31 Siku hiyo waliwashambulia Wafilisti kutoka Mikmashi
hadi Aiyaloni. Na watu walikuwa wamechoka sana. 32 Hivyo watu wakazivamia
nyara na kuchukua kondoo, ng'ombe na ndama na kuwachinja hapo chini. Watu
walikula nyama zao pamoja na damu. 33 KIsha wakamwambia Sauli, “Tazama,
watu wanamtenda BWANA dhambi kwa kula pamoja na damu.” Sauli akasema,
“Mmetenda isivyo haki. Sasa, viringisheni jiwe kubwa kwangu.” Sauli akasema,

34 “Nendeni kati watu, na muwaambie, 'Kila mtu alete ng'ombe na kondoo wake,
wawachinje hapa, na kuwala. Msimtende BWANA dhambi kwa kula na damu.”'
Kwa hiyo watu wote wakaleta kila mtu na ng'ombe wake usiku huo na kuwachinja
mahali hapo. 35 Sauli akamjengea BWANA madhabahu, ambayo ilikuwa ya kwanza
kwake kumjengea BWANA. 36 Ndipo Sauli akasema, “Haya tuwafukuze Wafilisti usiku
na kuwateka nyara hadi asubuhi; tusimwache hata mtu mmoja akiwa hai.” Nao
wakamjibu, “Fanya unaloona linakupendeza.” Lakini kuhani akasema, “Hebu na
tumkaribie Mungu mahali hapa.” 37 Sauli alitaka kumuuliza Mungu maswali zaidi,
“Je, inanipasa kuwafukuza Wafilisti? Je, utawaweka katika mkono wa Israeli?” Lakini
siku hiyo BWANA hakumjibu kitu. 38 Ndipo Sauli akasema, “Njoni hapa, viongozi
wote wa watu; mjue na kuona jinsi dhambi hii ilivyotokea leo. 39 Kwa maana, kama
BWANA aishivyo, aliyewaokoa Israeli, hata kama angekuwa mwanangu Yonathani,
atapaswa kufa.” Lakini hakuna hata mtu mmoja miongoni mwa watu aliye mjibu
neno. 40 Basi akawaambia Waisraeli wote, “Simameni upande mmoja, na mimi
na Yonathani tutasimama upande mwingine.” Kisha watu wakamwambia Sauli,
“Fanya lile unaloona jema kwako.” 41 Kwa hiyo, Sauli akamwambia BWANA, Mungu
wa Israeli, “Tuoneshe Thumimu.” Yonathani na Sauli wakatwaliwa, lakini watu
walinusurika kuchaguliwa. 42 Basi Sauli akasema, “Tupa mawe ya bahati nasibu
tuone kati yangu na mwanangu Yonathani.” Ndipo Yonathani akatwaliwa. 43 Kisha
Sauli akamwambia Yonathani, “Niambie umefanya nini.” Yonathani akamwambia
baba yake, “Nilionja asali kidogo kwa kutumia ncha ya fimbo iliyokuwa mkononi
mwangu. Niko hapa; Nitakufa.” 44 Sauli akasema, “Mungu afanye hivyo na kuzidi
hata kwangu, kama Yonathani hautakufa.” 45 Basi watu wakamuuliza Sauli, “Je,
inampasa Sauli afe, ni nani aliyetekeleza ushindi huu mkubwa kwa ajili ya Israeli?
Mbali na hayo! Kama BWANA aishivyo, hata unywele mmoja wa kichwa chake
hautaanguka chini, kwa maana leo amefanya kazi pamoja na Mungu.” Hivyo hao
watu walimuokoa Yonathani ili asife. 46 Basi Sauli akasita kuwafuatia Wafilisti, nao
wakarudi katika makao yao. 47 Sauli alipoanza kutawala juu ya Israeli, alipigana na
adui zake wote kila upande. Alipigana dhidi ya Moabu, dhidi ya watu wa Amoni,
Edomu, wafalme wa Zoba, na Wafilisti. Popote alipogeukia aliwapiga kwa adhabu
adui zake. 48 Alitenda kwa ushujaa mkubwa na kuwashinda Waamaleki. Aliwaokoa
Israeli kutoka mikono ya watu ambao waliwateka nyara. 49 Basi wana wa Sauli
walikuwa ni hawa Yonathani, Ishvi, na Malkishua. Na majina ya binti zake wawili
yalikuwa ni haya, Merabu mzaliwa wa kwanza, na mdogo aliitwa Mikali. 50 Jina la
mke wa Sauli aliitwa Ahinoamu; naye alikuwa binti Ahimaasi. Na jina la Jemedari
wa jeshi lake aliitwa Abneri mwana wa Neri, baba mdogo wa Sauli. 51 Kishi alikuwa
baba yake Sauli; na Neri alikuwa baba yake na Abneri, wote walikuwa wana wa
Abieli. 52 Kulikuwa na mapigano makali dhidi ya Wafilisti katika siku zote za Sauli.
Naye alipomwona mtu yeyote mwenye nguvu, au mtu yeyote jasiri, alimuunganisha
kwake.

# 15

1 Samweli akamwambia Sauli, “BWANA alinituma nikutie mafuta uwe mfalme wa
watu wake Israeli. Basi sikiliza maneno ya BWANA. 2 Hivi ndivyo BWANA wa majeshi
asemavyo, 'Nilichunguza jinsi Amaleki alivyomfanyia Israeli kwa kuwapinga njiani,
walipopanda kutoka Misri. 3 Sasa nenda umshambulie Amaleki na ukaangamize
kabisa vitu vyote walivyo navyo. Usiwaache, ua wote mwanamme na mwanamke,
mtoto na mtoto mchanga, ng'ombe na kondoo, ngamia na punda.”' 4 Sauli
akwaita watu na kuwahesabu katika mji wa Talemu: watu mia mbili elfu waendao
kwa miguu, na watu elfu kumi kutoka Yuda. 5 Kisha Sauli akaja hadi mji wa

Amaleki akangoja huko bondeni. 6 Ndipo Sauli akawaambia Wakeni, “Nendeni,
muondoke, mkajitenge na Waamaleki, nisije kuwaangamiza pamoja nao. Kwa maana
ulionesha wema kwa watu wote wa Israeli, walipotoka Misri.” Kwa hiyo Wakeni
wakajitenga na Waamaleki. 7 Kisha sauli akawashambulia Waamaleki, kutoka
Havila hadi kufika Shuri, ulio mashariki mwa Misri. 8 Basi akamchukua Agagi
mfalme wa Waamaleki akiwa hai; aliwaangamiza kabisa watu wote kwa ncha ya
upanga. 9 Lakini Sauli na watu wake wakamwacha Agagi akiwa hai, pamoja na
kondoo wazuri, ng'ombe, ndama wanono, na wanakondoo. Kila kitu kilichokuwa
kizuri, hawakukiangamiza. Bali waliangamiza kabisa chochote kilichodharaulika
na kisicho na thamani. 10 Baadaye neno la BWANA likamjia Samweli, kusema,
11 “Inanihuzunisha kwamba nimemchagua Samweli awe mfalme, kwa maana
aligeuka nyuma asinifuate na hakutekeleza maagizo yangu.” Samweli alikasirika;
akamlilia BWANA usiku kucha. 12 Samweli aliamka mapema akutane na Sauli
wakati wa asubuhi. Samweli aliambiwa, “Sauli alifika Karmeli na amejijengea
ukumbusho kwa ajili yake, kisha aligeuka na kuendelea chini hadi Gilgali.” Ndipo
13 Samweli akamwendea Sauli, na Sauli akamwambia, “Umebarikiwa na BWANA!
Nami nimetekeleza amri ya BWANA.” 14 Samweli akasema, “Hicho kilio cha kondoo
ni cha nini basi masikioni mwangu, na hiyo milio ya ng'ombe ninayosikia? 15 Sauli
akamjibu, “Wao wamewaleta kutoka kwa Waamaleki. Kwa sababu watu waliwaacha
hai kondoo wazuri na ng'ombe, kwa ajili ya sadaka kwa BWANA Mungu wako.
Zilizobaki tuliziangamiza kabisa.” 16 Ndipo Samweli akamwambia Sauli, “Subiri
nitakumbia kile ambacho BWANA amekisema kwangu usiku.” Sauli akamwambia,
“Sema!” 17 Samweli akasema, “Ingawa wewe ni mdogo machoni pako mwenyewe,
je, hukufanywa mkuu wa kabila za Israeli? Na BWANA akakutia mafuta uwe mfalme
juu ya Israeli; 18 BWANA alikutuma katika safari yako akisema, 'nenda na uangamize
kabisa wenye dhambi, Waamaleki, na upigane dhidi yao hadi wameangamizwa.'
19 Kwa nini basi haukuitii sauti ya BWANA, bali badala yake ulishikilia nyara
na ukafanya uovu machoni pa BWANA?” 20 Ndipo Sauli akamwambia Samweli,
“Kweli kabisa niliitii sauti ya BWANA, Na nimeifuata njia ambayo BWANA alinituma.
Nimemteka Agagi, mfalme wa Waamaleki, na kuwaangamiza kabisa Waamaleki.
21 Lakini watu walichukua baadhi ya nyara-kondoo na ng'ombe, na vitu vizuri
vilivyokusudiwa kuangamizwa, ili wavitoe dhabihu kwa BWANA, Mungu wako, huko
Gilgali.” 22 Samweli akajibu, “Je, BWANA hufurahia sadaka za kuteketezwa na
dhabihu kama ilivyo kuitii sauti yake? Utii ni bora kuliko dhabihu, na kusikia ni
bora kuliko mafuta ya beberu. 23 Kwa maana uasi ni sawa na dhambi ya uchawi, na
ukaidi ni sawa na uovu na udhalimu. Kwa kuwa umelikataa neno la BWANA, naye
pia amekukataa usiwe mfalme.” 24 Ndipo Sauli akamwambia Samweli, “Nimetenda
dhambi; kwa maana nimevunja amri ya BWANA na maneno yako, kwa sababu
niliwaogopa watu na kuitii sauti yao. 25 Sasa, tafadhali nisamehe dhambi yangu,
na urudi nami ili nipate kumcha BWANA.” 26 Samweli akamwambia Sauli, “Sitarudi
pamoja na wewe; kwa sababu umekataa neno la BWANA, naye BWANA amekukataa
usiwe mfalme juu ya Israeli.” 27 Samweli alipogeuka kuondoka, Sauli akashika pindo
la kanzu yake, na likachanika. 28 Samweli akamwambia, “BWANA ameuchana ufalme
wa Israeli kutoka kwako leo na amempa ufalme huo jirani yako, aliye bora kuliko
wewe. 29 Pia, yeye ni Uwezo wa Israeli hatasema uongo wala kubadili nia yake;
kwa sababu si mwanadamu, kwamba abadili nia yake.” 30 Kisha Sauli akasema,
“Nimetenda dhambi. Lakini tafadhali nipe heshima wakati huu mbele ya wakuu
wa watu wangu na mbele ya Israeli. Urudi tena pamoja nami, kusudi niweze
kumcha BWANA, Mungu wako.” 31 Hivyo Samweli akamrudia tena Sauli, na Sauli
akamcha BWANA. 32 Kisha Samweli akasema, “Mmlete hapa kwangu Agagi mfalme

wa Waamaleki." Agagi akafika kwake akiwa amefungwa minyororo na kusema,
"Hakika uchungu wa kifo umepita." 33 Naye Samweli akamjibu, "Jinsi upanga wako
ulivyofanya wanawake wapoteze watoto, vivyo hivyo mama yako naye hatakuwa na
mtoto miongoni mwa wanawake." Kisha Samweli akamkata Agagi vipande vipande
mbele za BWANA huko Gilgali. 34 Samweli akaenda Rama, na Sauli akapanda kwenda
nyumbani kwake Gibea ya Sauli. 35 Samweli hakumuona tena Sauli hadi siku ya kifo
chake, lakini alimwombolezea Sauli. Na BWANA alijuta kwa kumfanya Sauli awe
mfalme juu ya Israeli.

# 16

1 BWANA akamwambia Samweli, "Utamlilia Sauli kwa muda gani, ikiwa
nimemkataa asiwe mfalme juu ya Israeli? Ijaze pembe yako mafuta na uende.
Nitakutuma kwa Yese akaaye Bethlehemu, maana nimejichagulia mfalme katika
wanawe. 2 Samweli akasema, "Jinsi gani nitaenda? Kama Sauli akisikia jambo
hili, ataniua." BWANA akasema, "chukua mtamba na useme, 'Nimekuja kutoa
dhabihu kwa BWANA.' 3 Umwite Yese aje kwenye dhabihu, nami nitakuonesha kile
utakachofanya. Utamtia mafuta kwa ajili yangu yule nitakaye kuambia." 4 Samweli
akafanya kama BWANA alivyosema na akaenda Bethlehemu. Wazee wa mji walikuwa
wakitetemeka walipokuja kuonana naye na wakasema, "Je, umekuja kwa amani?"
5 Naye akasema, "kwa amani; Nimekuja kutoa dhabihu kwa BWANA. Jitoeni wenyewe
kwa BWANA kwa ajili ya dhabihu na muandamane nami," Na akamweka wakfu
Yese na watoto wake kwa BWANA, na baadaye aliwaita wote kwenye dhabihu.
6 Walipofika, akamwangalia Eliabu na akajisemea mwenyewe kwamba mtiwa mafuta
wa BWANA hakika amesimama mbele yake. 7 Lakini BWANA akamwambia Samweli,
"Usimwangalie sura yake ya nje, au kimo cha umbo lake; kwa sababu nimemkataa.
Maana BWANA haangalii kama mtu aangaliavyo; mtu hutazama sura ya nje, bali
BWANA huutazama moyo." 8 Kisha Yese akamwita Abinadabu akamwambia apite
mbele ya Samweli. Na Samweli akasema, "Hata huyu BWANA hakumchagua." 9 Kisha
Yese akmwambia Shama apite karibu. Na Samweli akasema, "Hata huyu BWANA
hakumchagua." 10 Yese akawaleta watoto wake saba wakapita mbele ya Samweli. Na
Samweli akamwambia Yese, "Hakuna hata mmoja aliyechaguliwa na BWANA kati ya
hawa." 11 Kisha Samweli akamuulia Yese, "Je, watoto wako wote wako hapa?" Naye
akajibu, "Yupo mdogo kabisa lakini anachunga kondoo." Samweli akamwambia Yese,
"Tuma watu wakamwite; maana hatutakaa chini hadi atakapofika hapa." 12 Yese
akawatuma watu wakamleta. Naye kijana huyu alikuwa mwekundu na mwenye
macho mazuri na mwenye muonekano mzuri. BWANA akasema, "Amka, umtie
mafuta; maana huyu ndiye." 13 Ndipo Samweli akachukua pembe yenye mafuta
na kumtia mafuta katikati ya kaka zake. Roho wa BWANA akamwijia Daudi kwa
nguvu tangu siku hiyo na kuendelea. Kisha Samweli akanyanyuka na kwenda Rama.
14 Basi Roho wa BWANA akamwacha Sauli, badala yake roho ya ubaya kutoka kwa
BWANA ikamsumbua. 15 Watumishi wa Sauli wakamwambia, "Tazama, roho ya
ubaya kutoka kwa Mungu inakusumbua. 16 Haya bwana wetu hebu sasa amuru
watumishi wako walio mbele yako wamtafute mtu mwenye ujuzi wa kupiga kinubi.
Basi ikwa roho wa ubaya kutoka kwa Mungu yuko juu yako, atakipiga kinubi nawe
utajisikia vizuri." 17 Sauli akawaambia watumishi wake, "Mnitafutie mtu anayeweza
kupiga vizuri na mmlete kwangu." 18 Ndipo kijana mmoja kati yao akajibu, na
kusema, "Nimemuona mtoto wa Yese Mbethtelehemu, aliye mjuzi katika kupiga, ni
mwenye nguvu, mtu jasiri, mtu wa vita, mwenye busara aongeapo, mtu mzuri kwa
uso; na BWANA yuko pamoja naye." 19 Hivyo Sauli akawatuma wajumbe kwa Yese, na
kusema, "Nitumie mtoto wako Daudi, anayewatunza kondoo." 1 Samweli! 6: 20-21

[20] Yese akamchukua punda aliyebeba mikate, na kiriba cha divai, na mwana-mbuzi,
na akamtuma kwa Sauli pamoja na vitu hivyo. [21] Ndipo Daudi akafika kwa Sauli
na kuanza kazi yake. Sauli alimpenda sana Daudi, na akawa mbeba silaha wake.
[22] Sauli akawatuma wajumbe kwa Yese, akisema, "Mruhusu Daudi awe mbele yangu,
maana amepata kibali machoni pangu." [23] Wakati wowote roho ya usumbufu kutoka
kwa Mungu ikiwapo juu ya Sauli, Daudi alichukuwa kinubi na kukipiga. Hivyo Sauli
angeburudishwa na kupona, na huyo roho wa usumbufu angemtoka.

# 17

[1] Basi Wafilisti walikusanya majeshi yao kwa ajili ya vita. Walikusanyika huko Soko,
iliyoko Yuda. Nao wakapiga kambi kati ya Soko na Aseka katika Efesdamimu. [2] Sauli
na watu wa Israeli alijikusanya na kuweka kambi katika bonde la Ela, na wakapanga
vita kukutana na Wafilisti. [3] Wafilisti walisimama juu ya mlima upande mmoja, na
Iraeli nao walisimama juu ya mlima upande mwingine wakitenganishwa na bonde
kati yao. [4] Mtu mmoja mwenye nguvu akatoka katika kambi ya Wafilisti, mtu huyo
aliitwa Goliathi wa Gathi, kimo chake mikono sita na shubiri moja. [5] Alikuwa na
chepeo ya shaba kichwani mwake, na alivaa dirii ya chuma. Hiyo dirii ilikuwa na
uzito wa shekeli elfu hamsini za shaba. [6] Alikuwa na mabampa ya shaba kwenye
miguu yake na mkuki wa shaba katikati ya mabega yake. [7] Ule mpini wa mkuki
wake ulikuwa mkubwa, wenye kamba iliyo na kitanzi kwa ajili ya kuutupia kama
kamba ya sindano ya mfumaji. Kichwa cha mkuki wake kilikuwa na uzito wa
shekeli mia sita za chuma. Aliyembebea ngao alitembea mbele yake. [8] Alisimama
akayapigia kelele majeshi ya Israeli, "Kwa nini mmekuja na mmejipanga kwa ajili
ya vita? Mimi si Mfilisti, na ninyi si watumishi wa Sauli? Chagueni mtu kutoka
kwenu ateremke na kuja kwangu. [9] Kama anaweza kupigana nami na kuniua,
hapo ndipo tutakuwa watumwa wenu. Lakini kama nitamshinda na kumuua, basi
mtakuwa watumwa wetu na kututumikia." [10] Mfilisti huyo akasema tena, "Leo
ninayapa changamoto majeshi ya Israeli. Mnipe mtu ili tuweze kupigana naye."
[11] Sauli na Israeli wote waliposikia alichosema Mfilisti huyo, walikata tamaa na
kuogopa sana. [12] Basi Daudi alikuwa mwana wa Mwefraimu wa Bethtelehemu ya
Yuda, aliyeitwa Yese. Naye alikuwa na watoto wanane wa kiume. Yese alikuwa
mtu mzee katika siku za Sauli, mwenye umri mkubwa kati ya watu. [13] Watoto
watatu wakubwa wa Yese walimfuata Sauli vitani. Majina ya watoto wake watatu
waliokwenda vitani yalikwa ni Eliabu mzaliwa wa kwanza, aliyemfuata Abinadabu,
na watatu aliitwa Shama. [14] Daudi ndiye aliyekuwa mdogo kabisa. Hao wakubwa
watatu walimfuata Sauli. [15] Basi Daudi alikwenda na kurudi akipita kati ya majeshi
ya Sauli akiwa na kondoo za baba yake huko Bethtelehemu, ili kuwachunga. [16] Kwa
muda wa siku arobaini yule Mfilisti mwenye nguvu alikuwa akijitokeza asubuhi na
jioni kwa ajili ya vita. [17] Kisha Yese akamwambia mwanawe Daudi, "Wapelekee
kaka zako efa ya bisi na hii mikate kumi, na uzipeleke upesi kule kambini kwa
ajili ya kaka zako. [18] Pia peleka hizi jibini kumi kwa jemedari wa kikosi chao cha
elfu. Ukawaangalie wako na hali gani kisha uniletee habari kuhusu wanavyoendelea
vizuri. [19] Kaka zako wako pamoja na Sauli na watu wote wa Israeli katika bonde
la Ela, wanapigana na Wafilisti." [20] Daudi aliamka asubuhi na mapema na kuliacha
kundi chini ya uangalizi wa mchungaji. Akachukua vile vitu na kuondoka, kama
Yese alivyomwamuru. Akafika kambini wakati jeshi linaondoka kwenda uwanja
wa vita wakipiga kelele za vita. [21] Nao Israeli na Wafilisti walijipanga kivita, jeshi
dhidi ya jeshi. [22] Daudi aliviacha vitu vyake kwa mtunza mahitaji, akalikimbilia
jeshi, na kuwasalimia kaka zake. [23] Alipoongea nao, yule mtu mwenye nguvu,
Mfilisti wa Gathi, jina lake Goliathi, akajitokeza kutoka majeshi ya Wafilisti, naye

akasema maneno yaleyale kama hapo mwanzo. Naye Daudi akayasikia. 24 Watu
wote wa Israeli walipomwona Goliathi, walimkimbia na waliogopa sana. 25 Watu wa
Israeli walisema, “Umemuona mtu huyu aliyejitokeza? Amekuja kuipa changamoto
Israeli. Basi mfalme atampa mali nyingi mtu atakayemua, atamuozesha binti yake,
na familia ya baba yake haitalipa kodi katika Israeli.” 26 Daudi akawauliza watu
waliosimama karibu naye, “Atafanyiwa nini mtu ambaye atamuua Mfilisti huyu
na kuiondolea Israeli fedheha? Ni nani Mfilisti huyu asiyetahiriwa ayatukanaye
majeshi ya Mungu aliye hai?” 27 Ndipo watu wakarudia kile walichokuwa wamesema
na kumwambia, “Ndivyo iitakavyofanyika kwa mtu atakayemuua.” 28 Kaka yake
mkubwa Eliabu, alisikia wakati akisema na watu. Hasira ya Eliabu ikawaka moto
dhidi ya Daudi, naye akamuuliza, “Kwa nini umekuja hapa? Wale kondoo wachache
umewaacha na nani huko nyikani? Nakijua kiburi chako, na utundu wa moyo
wako; maana umekuja hapa ili uweze kuona mapigano.” 29 Naye Daudi akamjibu,
“Nimefanya nini sasa? Mimi si nuliuliza swali tu? 30 Akamgeukia mtu mwingine
na kumwacha huyo, na kusema vivyo hivyo. Nao watu wakajibu vilevile kama
mwanzo. 31 Maneno aliyosema Daudi yaliposikika, askari waliyasema tena kwa
Sauli, naye akawatuma kwa Daudi. 32 Kisha Daudi akamwambia Sauli, “Pasiwepo
moyo wa mtu atakayezimia kwa sababu ya Mfilisti huyo; Mtumishi wako atakwenda
kupigana na Mfilisti huyu.” 33 Sauli akamwambia Daudi, “Huwezi kumpinga Mfilisti
ama kupigana naye; wewe ni kijana tu, na yeye amekuwa mtu wa vita tangu ujana
wake.” 34 Lakini Daudi akamwambia Sauli, “Mtumishi wako alikuwa akichunga
kondoo za baba yake. Mara simba au dubu alikuja akamchukua mwana kondoo
kutoka kundini, 35 Nilimfukuza na kumshambulia na kumpokonya kutoka kinywani
mwake. Na aliponirukia, nilimshika ndevu zake, nilimpiga, na kumuua. 36 Mtumishi
wako amekwisha kmuua simba na dubu. N huyu Mfilisti asiyetahiriwa atakuwa
kama mmoja wa wanyama hao, kwa kuwa ameyadharau majeshi ya Mungu aliye
hai.” 37 Daudi akasema, “BWANA aliyeniokoa kutoka makucha ya simba na makucha
ya dubu. Ataniokoa kutoka mkono wa Mfilisti huyu.” Kisha Sauli akamwambia
Daudi, “Nenda, BWANA awe pamoja nawe.” 38 Sauli akamvika Daudi vazi lake la
vita. Akamvika chepeo ya shaba kichwani pake, na akamvika koti la chuma. 39 Daudi
akaufunga upanga wake juu ya vazi la Sauli. Lakini hakuweza kutembea, kwa sababu
hakupata mafunzo kwa mavazi hayo. Ndipo Daudi akamwambia Sauli, “Siwezi
kwenda kupigana nikiwa na haya, maana sikupata mafunzo kwa haya.” Kwa hiyo
Daudi akayavua. 40 Akachukua fimbo mkononi mwake na akachagua mawe matano
laini kutoka katika kijito; akayaweka kwenye mfuko wake wa kichungaji. Kombeo
lake lilikuwa mkononi akawa anamsogelea yule Mfilisti. 41 Yule Mfilisti akaja na
kumsogelea Daudi, mbeba ngao yake akiwa mbele yake. 42 Mfilisti alipotazama kila
upande na kumuona Daudi, akamdharau, maana alikuwa kijana tu, mwekundu, na
umbo la kupendeza. 43 Ndipo Mfilisti akamuuliza Daudi, “Je, mimi ni mbwa, hata
ukanijia na fimbo? Naye Mfilisti kwa miungu yake akamlaani Daudi. 44 Huyo Mfilisti
akamwambia Daudi, “Njoo kwangu, na nyama yako nitawatupia ndege wa angani
na wanyama wa mwituni.” 45 Daudi akamjibu Mfilisti, “Unaniijia kwa upanga, kwa
mkuki na mkuki mdogo. Bali mimi nakuijia kwa jina la BWANA wa majeshi, Mungu
wa Majeshi ya Israeli, uliyemdharau. 46 Leo BWANA atanipa ushindi dhidi yako,
na nitakuua na kukiondoa kichwa chako kwenye kiwiliwili. Leo nitawapa ndege wa
angani na wanyama wa mwituni walioko duniani mizoga ya jeshi la Wafilisti, ili dunia
yote ijue kwamba yupo Mungu katika Israeli, 47 na kusanyiko hili lote lijue kwamba
BWANA hatoi ushindi kwa upanga wala kwa mkuki. Kwa kuwa vita ni ya BWANA,
na atawaweka katika mkono wetu.” 48 Mfilisti aliponyanyuka na kukaribia akutane
na Daudi, ndipo Daudi akakimbia kwa haraka kuelekea jeshi la adui ili akutane naye.

49 Daudi aliweka mkono wake mfukoni, akachukua jiwe kutoka humo, akalitupa
kwa kombeo, na likampiga Mfilisti kwenye paji la uso, akaanguka chini kifudifudi.
50 Daudi alimshinda Mfilisti kwa kombeo na kwa jiwe moja. Alimpiga huyo Mfilisti
na kumuua. Mkononi mwa Daudi hakukuwa na upanga. 51 Ndipo Daudi akakimbia
akasimama juu ya Mfilisti na kutwaa upanga wake, akauchomoa kutoka alani,
akamuua, na kukata kichwa chake kwa upanga huo. 52 Ndipo watu wa Israeli na wale
wa Yuda wakaamka kwa kelele, na kuwafukuza Wafilisti kuvuka bonde na malango
ya Ekroni. Na maiti za Wafilisti walilala katika njia iendayo Shaaraimu, na njia yote
kuelekea Gathi na Ekroni. 53 Watu wa Israeli wakarejea kutoka kuwafukuza Wafilisti,
na wakateka nyara kambi yao. 54 Daudi akachukua kichwa cha Mfilisti na kukipeleka
Yerusalemu, lakini akaliweka vazi la vita katika hema lake. 55 Sauli alipomuona
Daudi akienda kukabiliana na yule Mfilisti, akamwambia Abneri, jemedari wa jeshi,
"Abneri, kijana huyu ni mtoto wa nani? Abneri akasema, "Kama uishivyo, mfalme,
mimi sijui." 56 Naye mfalme akasema, "Waulize wanaoweza kufahamu, mvulana
huyu ni kijana wa nani." 57 Daudi aliporudi kutoka kumuua yule Mfilisti, Abneri
alimchukuwa, na kumleta mbele ya Sauli akiwa na kichwa cha Mfilisti mkononi
mwake. 58 Sauli akamuuliza, "Kijana, wewe ni mtoto wa nani? Na Daudi akamjibu,
"Mimi ni mtoto wa mtumishi wako Yese Mbethlehemu."

# 18

1 Daudi alipokuwa amemaliza kuongea na Sauli, roho ya Yonathani ilishikana
na roho ya Daudi, na Yonathani akampenda kama roho yake mwenyewe. 2 Sauli
akamweka kazini Daudi siku hiyo, hakumwacha arudi nyumbani kwa baba yake.
3 Kisha Yonathani na Daudi wakafanya makubaliano ya urafiki kwa sababu Yonathani
alimenda kama roho yake mwenyewe. 4 Yonathani akavua kanzu aliyokuwa amevaa
na kumpa Daudi, akampa na vazi lake la kivita, pamoja na upanga, upinde, na mshipi.
5 Daudi alikwenda popote ambapo Sauli alimtuma, naye alifanikiwa. Sauli akamteua
Daudi awe mkuu wa wapiganaji. Jambo hili lilipendeza machoni pa watu na katika
macho ya watumishi wa Sauli. 6 Wakati wanarudi nyumbani kutoka kuwapiga
Wafilisti, wanawake walitoka miji yote ya Israeli, wakiimba na kucheza, ili kukutana
na mfalme Sauli, wakiwa na matowazi, wenye furaha, na wakiwa na ala za muziki.
7 Hao wanawake waliimba kwa kupokezana huku wakicheza; Wakiimba: "Sauli
ameua maelfu yake, Na Daudi ameua makumi elfu yake." 8 Sauli alikasirika sana,
na wimbo huu haukumpendeza. Naye akasema, "Wamemsifia Daudi juu ya makumi
elfu, lakini wamenisifia melfu tu mimi! Atapata kitu gani zaidi isipokuwa ufalme?
9 Kuanzia siku hiyo na kuendelea, Sauli alimuangalia Daudi kwa mashaka. 10 Kesho
yake yule roho ya ubaya kutoka kwa Mungu ikamwingia Sauli kwa nguvu. Naye
akawa anafanya kama mwendawazimu nyumbani mwake. Hivyo Daudi akapiga
kifaa chake, kama alivyofanya kila siku. Sauli alikuwa na mkuki wake mkononi.
11 Sauli akatupa mkuki wake, kwani alifikiri, "Nitampigilia ukutani." Lakini Daudi
mara mbili aliepa uwepo wa Sauli. 12 Sauli alimwogopa Daudi, kwa sababu BWANA
alikuwa pamoja naye, lakini hakuwa na Sauli tena. 13 Hivyo Sauli alimuondoa Daudi
mbele yake na akamteua kuwa kamanda wa kikosi cha askari elfu moja. Kwa namna
hii David alitoka na kuingia mbele ya watu. 14 Daudi alikuwa akistawi kwa mambo
yake yote, maana BWANA alikuwa pamoja naye. 15 Sauli alipoona kwamba Daudi
anastawi, alimwogopa. 16 Lakini Israeli yote na Yuda walimpenda Daudi, maana
alitoka na kuingia mbele yao. 17 Kisha Sauli akamwambia Daudi, "Huyu hapa ni
binti yangu mkubwa Merabu. Nitakupatia awe mke wako. Ila tu uwe jasiri kwa
ajili yangu na upigane vita vya BWANA." Maana Sauli alifikiri, "Usije mkono wangu
ukawa juu yake, ila acha mkono wa Wafilisti uwe juu yake." 18 Daudi akamwambia

Sauli, “Mimi ni nani, na maisha yangu yana nini, au hata maisha ya familia ya
baba yangu katika Israeli, kiasi cha kuwa mkwe wa mfalme?” 1 Samweli 18-19-
19 [19] Lakini wakati ambao Merabu, binti Sauli, ilipasa kuwa ameolewa na Daudi,
aliozwa kwa Adrieli Mmeholathi. [20] Lakini Mikali, binti Sauli, alimpenda Daudi.
Na watu walimwambia Sauli, na jambo hilo likampendeza. [21] Ndipo Sauli akafikiri,
“Nitampatia huyu awe mke wake, ili uwe mtego kwake, na hivyo mkono wa Wafilisti
pengine uwe juu yake.” Kwa hiyo Sauli akamwambia Daudi mara ya pili, “Wewe
utakuwa mkwe wangu.” [22] Sauli akawaamuru watumishi wake, “Ongeeni na Daudi
kwa njia ya siri, na mseme, 'Tazama, mfalme anakufurahia, na watumishi wake wote
wanakupenda. Sasa basi, uwe mkwe wa mfalme.'” [23] Hivyo watumishi wa Sauli
wakayasema maneno haya kwa Daudi. Na Daudi akasema, “Kwenu ninyi mnaona
ni jambo dogo kuwa mkwe wa mfalme, mimi ni maskini, na heshima yangu ni
ndogo.” [24] Watumishi wa Sauli wakarudisha kwake taarifa ya maneno ambayo Daudi
aliyasema. [25] Na Sauli akasema, “Hivi ndivyo mtakavyo mwambia Daudi, 'Mfalme
haitaji mahari yoyote, isipokuwa govi mia moja za Wafilisti, ili ajilipize kisasi kwa
adui wa mfalme.”' Basi Sauli alifikiri atamwangusha Daudi kwa mkono wa Wafilisti.
[26] Watumishi wake walipomwambia maneno haya, yakamvutia Daudi awe mkwe
wa mfalme. [27] Kabla siku hizo hazijapita, Daudi aliondoka na watu wake na kuwaua
Wafilisti mia mbili. Daudi akazileta govi zao, na kumkadhi mfalme kulingana na idadi
yake, ili aweze kufanyika mkwe wa mfalme. Kwa hiyo Sauli akamwoza Mikali, binti
yake, awe mkewe. [28] Basi Sauli aliona na kufahamu kwamba BWANA alikuwa pamoja
na Daudi. Mikali, binti Sauli, akampenda Daudi. [29] Sauli akazidi kumwogopa Daudi.
Sauli akawa adui wa Daudi daima. [30] Ndipo wakuu wa Wafilisti wakajitokeza kwa
ajili ya vita, na mara zote walipojitokeza Daudi alifanikiwa zaidi kuliko watumishi
wote wa Sauli, hivyo jina lake likapata heshima kubwa.

# 19

[1] Sauli akamwambia Yonathani mwanawe na watumishi wake wote kwamba
wanapaswa kumuua Daudi. Lakini Yonathani, mwana wa Sauli, alitamani sana
akae na Daudi. [2] Hivyo Yonathani akamwambia Daudi, “Baba yangu Sauli anatafuta
kukuua. Kwa hiyo uwe macho wakati wa asubuhi na jifiche mahali pa siri.
[3] Nami nitatoka nje na kusimama kando ya baba yangu huko shambani uliko
wewe, na nitazungumza na baba yangu kuhusu wewe. Kama nikijua jambo lolote
nitakuambia.” [4] Yonathani alimsifia Daudi mbele ya Sauli baba yake akisema,
“Mfalme asije akafanya dhambi dhidi ya mtumishi wake Daudi. Maana yeye
hajakutenda dhambi, mambo aliyofanya yamekusaidia sana. [5] Maana alijitoa maisha
yake na kumuua yule Mfilisti, naye BWANA akawaletea Waisraeli wote wokovu
mkuu. Tena uliuona na kufurahi. Kwa nini utende dhambi juu damu isiyo na
hatia kwa kumuua Daudi bila sababu?” [6] Sauli alimsikiliza Yonathani. Sauli akaapa,
“Kama BWANA aishivyo, Yonathani hatauawa.” [7] Ndipo Yonathani akamwita Daudi
na kumwambia mambo hayo yote. Na Yonathani akamleta Daudi kwa Sauli, naye
Daudi akawa mbele zake kama zamani. [8] Baadaye kukawa na vita tena. Daudi
akatoka na kupigana na Wafilisti na kuwashinda kwa mauaji makubwa mno. Nao
wakakimbia mbele yake. [9] Yule roho wa ubaya kutoka kwa BWANA ikamjia Sauli
alipokuwa ameketi nyumbani mwake na mkuki mkononi mwake, na Daudi akiwa
anapiga chombo chake. [10] Sauli alijaribu kumpigilia Daudi ukutani kwa mkuki wake,
lakini akaponyoka kutoka machoni pake, na kwamba Sauli akashindilia mkuki ndani
ya ukuta. Daudi alikimbia na kutoroka usiku huo. [11] Bado Sauli aliwatuma wajumbe
nyumbani kwa Daudi wamvizie kusudi aweze kumuua asubuhi. Mkewe Daudi,
Mikali, akamwambia, “Usipoyaokoa maisha yako usiku huu, kesho utauwawa.”

12 Hivyo Mikali akamteremsha Daudi kupita dirishani. Naye akaenda, akakimbia
na kutoroka. 13 Mikali alichukua kinyago na kukilaza juu ya kitanda. Kisha akaweka
mto wa singa za mbuzi kichwani pake, na akakifunika na nguo. 14 Sauli alipowatuma
wajumbe kumchukua Daudi, mkewe akasema, “ Daudi ni mgonjwa.” 15 Kisha
Sauli akawatuma wajumbe kumtazama; akisema, “Mleteni kwangu akiwa kitandani,
ili nimuue.” 16 Wale wajumbe walipoingia ndani, tazama, kile kinyago kilikuwa
kitandani pamoja na mto wa singa za mbuzi kichwani. 17 Sauli akamuuliza Mikali,
“Kwa nini umenidanganya na kumwachilia adui yangu aende, na tena ametoroka?”
Mikali akamjibu Sauli, “Aliniambia, 'Acha niende. Kwa nini nikuuwe?”' 18 Basi Daudi
akakimbia na kutoroka, na akaenda kwa Samweli huko Rama na kumweleza yote
ambayo Sauli amemtendea. Ndipo yeye na Samweli wakaenda na kukaa Nayothi.
19 Naye Sauli akaambiwa kwamba, “Tazama, Daudi yuko huko Nayothi iliyoko Rama.”
20 Kisha Sauli akawatuma wajumbe kumkamata Daudi. Nao walipowaona kundi la
manabii wakitabiri, na Samweli akisimama kama kiongozi wao, Roho wa Mungu
akawaingia wale wajumbe wa Sauli, nao pia wakatabiri. 21 Sauli alipoambiwa
hivyo, akawatuma wajumbe wengine, nao pia wakatabiri. Basi Sauli aliwatuma tena
wajumbe kwa mara ya tatu, na hao pia wakatabiri. 22 Kisha naye akaenda Rama
na kufika katika kisima kirefu kilichoko huko Seku. Akauliza, “Samweli na Daudi
wako wapi?” Mtu mmoja akasema, “Angalia, Wako Nayothi huko Rama.” 23 Hivyo
Sauli akaenda Nayothi huko Rama. Ndipo Roho wa Mungu pia akaja juu yake, naye
alipokuwa akienda alitabiri, hadi alipofika Nayothi huko Rama. 24 Na yeye pia,
alirarua mavazi yake, naye pia akatabiri mbele ya Samweli siku hiyo akilala uchi
mchana kutwa na usiku kucha. Kwa sababu ya jambo hili, watu husema, “Je, Sauli
pia ni miongoni mwa manabii?”

# 20

1 Kisha Daudi akakimbia kutoka Nayothi huko Rama akaenda na kumwambia
Yonathani, “Nimefanya nini? Uovu wangu ni upi? Dhambi yangu ni ipi kwa baba
yako, inayofanya atafute kuutoa uhai wangu.” 2 Yonathani akamwambia Daudi, “La
hasha; hautakufa. Baba yangu hafanyi jambo kubwa wala dogo bila kunijulisha. Kwa
nini inamlazimu baba yangu anifiche jambo hili? La, siyo hivyo?” 3 Bado Daudi aliapa
tena na akasema, “Baba yako anajua wazi kwamba nimepata kibali machoni pako.
Pengine anasema, 'Asije Yonathani akajua jambo hili, labda atahuzunika.' Lakini
kweli kama BWANA aishivyo, kama wewe uishivyo, kuna hatua moja tu kati yangu na
mauti.” 4 Kisha Yonathani akamwambia Daudi, “Lolote utakalosema, nitakufanyia.”
5 Daudi akamwambia Yonathani, “Kesho ni siku ya mwezi mpya, na inanibidi kukaa
na kula pamoja na mfalme. Lakini acha niende, ili niweze kujificha katika shamba
hadi siku ya tatu jioni. 6 Baba yako akinikosa kabisa, ndipo utasema, 'Daudi aliniomba
kwa msisitizo ruhusa aondoke kwenda mjini kwake Bethlehemu; kwa sababu huko
ni kipindi cha utoaji wa dhabihu ya mwaka kwa familia yao yote.' 7 Kama atasema
kuwa ni vyema, 'basi mtumishi wako atakuwa na amani. Lakini kama atakasirika
sana, ndipo utajua kwamba ameamua kunitendea uovu. 8 Kwa hiyo, umtendee
wema mtumishi wako. Kwa maana umemweka mtumishi katika agano la BWANA
pamoja na wewe. Lakini kama kuna dhambi ndani yangu, wewe mwenyewe uniuwe;
maana kwa nini basi unipeleke kwa baba yako?” 9 Yonathani akasema, “La hasha!
Ikiwa ninajua kwamba baba ameamua baya likupate, siwezi kukuambia?” 10 Ndipo
Daudi akamwambia Yonathani, “Ni nani ataniambia ikiwa imetokea, baba yako
akakujibu kwa ukali?” 11 Yonathani akamwambia Daudi, “Njoo, hebu twende huko
shambani.” Ndipo wote wakaondoka kwenda shambani. 12 Yonathani akamwambia
Daudi, “Na BWANA, Mungu wa Israeli, awe shahidi. Kesho muda kama huu, nitakuwa

nimemuuliza baba yangu, au siku ya tatu, tazama, ikiwa kutakuwa na jambo zuri
upande wa Daudi; je, nisikutumie taarifa na kulidhihirisha kwako? 13 Na kama
ikimpendeza baba yangu akufanyie madhara, Basi BWANA ayafanye hayo kwa
Yonathani na kuzidi ikiwa sitakujulisha jambo na kukupeleka mbali, ili kwamba
uende kwa amani. Na BWANA awe pamoja nawe, kama alivyokuwa na baba yangu.
14 Kama bado nikiwa hai, hautanionesha uaminifu wa agano la BWANA, kwamba
siwezi kufa? 15 Na usivunje kabisa uaminifu wako wa agano kati yako na nyumba
yangu, hata wakati BWANA atakapowaodoa kila mmoja wa adui za Daudi kutoka uso
wa dunia." 16 Basi Yonathani akafanya agano na nyumba ya Daudi na kusema, "Naye
BWANA atawaondoa maadui wa Daudi." (KISWAHILI IDIOM? ==== ULB ENGLISH
IDIOM) 17 Yonathani akamtaka Daudi aape tena kwa sababu ya upendo aliokuwa nao
juu yake, kwa sababu alimpenda kama alivyopenda roho yake mwenyewe. 18 Kisha
Yonathani akamwambia Daudi, "Kesho ni siku ya mwezi mpya. Hautakuwapo, kwa
sababu kiti chako kitakuwa wazi. 19 Utakapokuwa umekaa huko siku tatu, uende
upesi hadi mahala ulipojificha mara ya kwanza, wakati shughuli ikifanyika, na ukaye
karibu jiwe Ezeli. 20 Nitatupa mishale mitatu pembeni mwa jiwe, kama vile ninalenga
kitu fulani. 21 Kisha nitamtuma kijana wangu na kumwambia, 'Nenda utafute hiyo
mishale.' Kama nitamwambia kijana hivi, 'Tazama, mishale iko upande huu wa
kwako; kaichukue," ndipo uje; maana hapo kutakuwa na usalama kwako na siyo
madhara, kama BWANA aishivyo. 22 "Lakini kama nikimwambia kijana hivi, 'Tazama,
mishale iko mbele yako,' ndipo utakapokwenda zako, maana BWANA ametaka uende
zako. 23 Kulingana na makubaliano ambayo mimi na wewe tumeongea, angalia,
BWANA yupo kati yangu na wewe milele.'" 24 Kwa hiyo Daudi akajificha mle
shambani. Pindi mwezi ulipoandama, mfalme aliketi chini ale chakula. 25 Mfalme
alikaa juu ya kiti chake, kama kawaida kwenye kiti karibu na ukuta. Yonathani
alisimama wima, na Abneri alikaa ubavuni mwa Sauli. Lakini nafasi ya Daudi ilikuwa
wazi. 26 Hata hivyo Sauli hakusema kitu siku hiyo, kwa sababu alifikiri, "Kuna jambo
limempata Daudi. Hayuko safi; hakika hayuko safi." 27 Lakini siku ya pili, siku moja
baada ya mwandamo wa mwezi, bado nafasi ya Daudi ilikuwa tupu. Ndipo Sauli
akamuuliza Yonathani mwanaye, "Kwa nini mwana wa Yese hakuja kwenye chakula,
jana na hata leo?" 28 Yonathani akamjibu Sauli, "Daudi aliomba kwangu ruhusa kwa
dhati ili aende Bethlehemu. 29 Alisema, 'Tafadhali niruhusu niende. Maana familia
yetu wanayo dhabihu huko mjini, na kaka yangu ameniagiza niwe huko. Basi kama
nimepata kibali machoni pako, tafadhali niruhusu niende nikawaone kaka zangu.'
Hakuja kwenye meza ya mfalme kwa sababu hii." 30 Ndipo hasira ya Sauli iliwaka
juu ya Yonathani, na akamwambia, "Wee mwana wa mwanamke mkaidi na muasi!
Wadhani kwamba sijui kuwa umemchagua Mwana wa Yese kwa ajili ya aibu yako,
na kwa aibu ya uchi wa mama yako? 31 Kwa kuwa mwana wa Yese anaishi duniani,
siyo wewe wala ufalme wako utakaoimarika. Sasa basi, tuma watu wamlete kwangu,
kwa sababu inampasa kufa." 32 Yonathani akamjibu Sauli baba yake, "Kwa sababu
gani inampasa kuuwawa? Amefanya nini?" 33 Ndipo Sauli akamtupia mkuki apate
kumuua. Kwa hiyo Yonatani akatambua kwamba baba yake alinuia kumuua Daudi.
34 Yonathani alitoka mezani akiwa na hasira kali bila kula chakula siku ya pili ya
mwezi, kwa sababu alimhuzunikia Daudi, na kwa sababu baba yake amemwaibisha.
35 Ikawa asubuhi, Yonathani akaenda huko shambani kama walivyoahidiana na
Daudi, akiwa pamoja na kijana wake. 36 Akamwambia yule kijana wake, "Kimbia
utafute ile mishale niliyoitupa." Na kijana alikimbia, akatupa mshale mwingine
mbele yake. 37 Kijana alipofika katika eneo ambapo mshale ulitua, ule alioutuma
Yonathani, akamwita tena kijana, na kusema, "Huo mshale hauko mbele yako?"
38 Kisha Yonathani akamwita yule kijana, "Upesi, harakisha, usikawie!" Hivyo kijana

wa Yonathani akaikusanya mishale na kurudi kwa bwana wake. 39 Lakini huyo kijana
hakujua lolote. Ni Yonathani na Daudi tu ndio walijua habari yenyewe. 40 Yonathani
akampa kijana wake silaha na kumwambia, "Nenda, uzipeleke mjini." 41 Punde tu
kijana alipoondoka, Daudi akasimama kutokea upande wa kusini, akiwa amelala
kifudifudi, akainama mara tatu. Walibusiana wao kwa wao na wote wakalia kwa
pamoja, Daudi akilia zaidi. 42 Yonathani akamwambia Daudi, "Nenda kwa amani,
kwa sababu wote tumeapa kwa jina la BWANA na tulisema, 'BWANA awe kati yangu
na wewe, na awe kati ya uzao wangu na uzao wako, milele.'" Kisha Daudi alisimama
na akaondoka, na Yonathani akarudi mjini.

# 21

1 Kisha Daudi akafika Nobu kumuona Ahimeleki kuhani. Ahimeleki akaja akutane
na Daudi huku akitetemeka na kumwambia, "Kwa nini uko peke yako huna mtu wa
kuambatana na wewe?" 2 Daudi akamjibu Ahimeleki kuhani, "Mfalme amenituma
kwa jambo maalum na ameniambia hivi, 'Asiwepo hata mtu mmoja anayejua
chochote kuhusu shughuli niliyokutuma, na kile nilichokuagiza.' Nimewaelekeza
vijana kwenda sehemu fulani. 3 Sasa basi chakula gani kinapatikana hapa? Nipatie
mikate mitano, au chochote kilichopo hapa." 4 Huyo Kuhani alimjibu Daudi
na kusema, "Hakuna mkate wa kawaida mkononi, lakini ipo mikate takatifu-
kama vijana hawajatembea na wanawake." 5 Daudi akamjibu kuhani, "Hakika
hatujatembea na wanawake kwa siku hizi tatu. Nilipoanza safari, miili ya vijana
iliwekwa wakfu kwa BWANA, ingawa ilikuwa safari ya kawaida. Je, si zaidi sana leo
miili yao ikawekwa wakfu kwa BWANA." 6 Hivyo kuhani akampa mikate iliyokuwa
imewekwa wakfu kwa BWANA. Maana haikuwepo mikate mingine hapo, isipokuwa
tu ile ya wonyesho, ambayo iliondolewa kutoka kwa BWANA, ili sehemu yake
iwekwe mikate ya moto, inapokuwa imeondolewa. 7 Basi siku hiyo mmoja wa
watumishi wa Sauli alikuwapo mahali hapo, ameshilkiliwa mbele za BWANA. Jina
la mtu huyo aliitwa Doegi Mwedomu, mkuu wa wachungaji wa Sauli. 8 Daudi
akamwambia Ahimeleki, "Je, hakuna hata mkuki wowote au upanga? Maana mimi
sikubeba upanga wangu wala silaha zangu, maana ile shughuli ya mfalme ilikuwa
ya muhimu." 9 Kuhani akasema, "Ule upanga wa Mfilisti Goliathi, uliyemuua katika
bonde la Ela, uko hapa umefunikwa katika nguo nyuma ya naivera. kama unataka
kuuchukua huo, uchukue, maana hakuna silaha nyingine hapa." Daudi akasema,
"Hakuna silaha nyingine kama hiyo, nipatie hiyo." 10 Daudi aliamka na kukimbia
mbali na Sauli na akaenda kwa Akishi, mfalme wa Gathi. 11 Mtumishi wa Akishi
akamwambia, "huyu siye Daudi mfalme wa nchi hii? Je, wanawake hawakupokezana
wakiimba na kucheza, 'Sauli ameua maelfu yake, na Daudi makumi elfu yake?"'
12 Daudi akayaweka maneno hayo moyoni mwake na akamwogopa sana Akishi,
mfalme wa Gathi. 13 Daudi akabadili mwenendo wake mbele yao na akajifanya kuwa
mwendawazimu machoni pao; akachora-chora alama kwenye vizingiti vya milango
huku akitiririsha mate yake chini ya ndevu zake. 14 Ndipo Akishi akawaambia
watumishi wake, "Tazameni, mnaona mtu huyu ni mwehu. 15 Kwa nini mmemleta
kwangu? Je, mimi nina haja na wehu, kumbe mmemleta mtu huyu ili anifanyie hayo
mbele yangu? Hivi kweli huyu ataingia nyumbani mwangu?

# 22

1 Basi Daudi aliondoka hapo na akatoroka kwenda kwenye pango la Adulamu.
Kaka zake na wote wa nyumba ya baba yake waliposikia hayo, wakateremka
kumwendea huko. 2 Kila mmoja aliyekuwa na mahangaiko, kila mmoja aliyekuwa
na deni, na kila mmoja ambaye hakuwa na furaha moyoni-wote walijikusanya

kwake, na Daudi akawa jemedari wao. Kulikuwa na wanaume wapatao mia
nne waliokuwa pamoja naye. [3] Kisha Daudi alitoka huko akaenda Mispa huko
Moabu. Akamwambia mfalme wa Moabu, “Tafadhali waruhusu baba na mama
yangu wakae kwako hadi hapo nitakapojua kitu gani ambacho Mungu atafanya
kwa ajili yangu.” [4] Basi akawaacha kwa Mfalme wa Moabu. Baba na mama yake
wakakaa na mfalme kwa muda wote ambao Daudi alikuwa kwenye ngome yake.
[5] Kisha nabii Gadi akamwambia Daudi, “Usikae tena katika ngome yako. Ondoka
na uende katika nchi ya Yuda.” Kwa hiyo Daudi akatoka hapo na akaenda katika
msitu wa Harethi. [6] Sauli akasikia kwamba Daudi amepatikana, akiwa pamoja
na watu aliokuwa nao. Wakati huo Sauli alikuwa akikaa Gibea chini ya mti wa
mkwaju huko Rama, akiwa na mkuki wake mkononi mwake, na watumishi wake
wote walikuwa wamesimama wamemzunguka. [7] Sauli akawaambia watumishi wake,
Sasa sikilizeni, watu wa Benyamini! Je, mwana wa Yese atawapa mashamba na
mashamba ya mizabibu? Je, atawafanya nyote kuwa majemedari wa maelfu na
majemedari wa mamia, [8] hata ninyi nyote mnapanga njama dhidi yangu? Hakuna
hata mmoja wenu anayenijulisha kwamba mwanangu anafanya agano na mwana
wa Yese. Hakuna hata mmoja wenu anayenionea huruma. Hakuna hata mmoja
wenu anayenijulisha kwamba mwanangu anamchochea mtumishi wangu Daudi awe
kinyume changu. Leo mejificha na ananisubiri ili anishambulie.” [9] Kisha Doegi
Mwedomu, aliyesimama karibu na watumishi wa Sauli, akajibu, Nilimwona mwana
wa Yese akienda Nobu, kwa Ahimeleki mwana wa Ahitubu. [10] Alimwomba BWANA
ili apate kumsaidia, na alimpatia mahitaji na upanga wa Goliathi, Mfilisti” [11] Kisha
Mfalme akamtuma mtu amwite kuhani Ahimeleki mwana wa Ahitubu na watu wote
wa nyumba ya baba yake, makuhani waliokuwa huko Nobu. Wote walifika mbele
ya mfalme. [12] Sauli akasema, “Sasa sikiliza, mwana wa Ahitubu,” Naye akajibu,
“Niko hapa, bwana wangu.” [13] Sauli akamwambia, “Kwa nini unapanga njama
dhidi yangu, wewe pamoja na mwana wa Yese, kwa kumpatia mikate, na upanga,
na umemwomba Mungu kusudi amsaidie Daudi, kusudi aniasi mimi, na kujificha
sehemu ya siri, kama alivyofanya leo?” [14] Ndipo Ahimeleki akamjibu mfalme na
kusema, “Je, ni nani miongoni mwa watumishi wako wote aliyemwaminifu kama
Daudi, ni nani mkwe wa mfalme na yuko juu ya walinzi wako, na mwenye heshima
nyumbani mwako? [15] Je, leo ni mara ya kwanza kwangu kumuomba Mungu apate
kumsaidia? Hapana! Mfalme usinilaumu mimi mtumishi wako kwa jambo lolote
wala jamaa zangu wote. Maana mimi mtumishi wako sijui lolote kuhusu kadhia
hii.” [16] Mfalme akamjibu, “Hakika utakufa, Ahimeleki, wewe na jamaa yote ya
nyumba ya baba yako.” [17] Mfalme akamwambia mlinzi aliyesimama karibu naye,
“Geuka na uwauwe makuhani wa BWANA. Kwa sababu wanamuunga mkono Daudi,
na sababu walijua kwamba alikimbia, lakini hawakunijulisha.” Lakini watumishi
wa mfalme hawakunyoosha mkono wao kuwaua makuhani wa BWANA. [18] Ndipo
mfalme akamwambia Doegi, “Geuka na uwauwe makuhani.” Hivyo Doegi Mwedomu
akageuka na kuwapiga makuhani; akawaua watu themanini na watano waliovaa
naivera ya kitani siku hiyo. [19] Kwa ncha ya upanga, aliupiga Nobu, mji wa
makuhani, akiwaua wanaume na wanawake, watoto na wanyonyao, ng'ombe na
punda na kondoo. Wote aliwaua kwa ncha ya upanga. [20] Lakini mmoja wa wana
wa Ahimeleki mwana wa Ahitubu, aliyeitwa Abiathari, aliponyoka na kukimbilia
kwa Daudi. [21] Abiathari akamwambia Daudi kwamba Sauli amewaua manabii
wa BWANA. [22] Daudi akamwambia Abiathari, “Nilifahamu kuwa siku hiyo, Doegi
Mwedomu alikuwa mahali pale, kwamba hakika angemwambia Sauli. Nina wajibika
kwa kifo cha kila mtu katika familia ya baba yako! [23] Kaa pamoja nami na usiogope.
Maana mtu anayetafuta roho yako anatafuta pia roho yangu. Utakuwa salama ukiwa

pamoja nami.”

# 23

1 Wakamwambia Daudi, “Tazama, Wafilisti wanaupiga Keila na wanapora nafaka
inayopurwa.” 2 Hivyo Daudi akamwomba BWANA kwa ajili ya msaada, na
akamuuliza,” Je, niondoke niwapige hawa Wafilisti? BWANA akamwambia Daudi,
“Nenda ukawapige Wafilisti na kuokoa Keila.” 3 Daudi akaambiwa na watu wake,
“Angalia, hapa Yuda tunaogopa. Je, si zaidi sana kama tutaenda Keila kupambana na
majeshi ya Wafilisti?” 4 Ndipo Daudi akamwomba BWANA kwa ajili ya msaada, bado
tena, BWANA akamjibu, “Amka, uteremke hadi Keila. Maana nitakupatia ushindi
dhidi ya Wafilisti.” 5 Daudi na watu wake wakaenda Keila na kupigana na Wafilisti.
Wakahamisha ng'ombe wao na kuwapiga kwa mauaji makubwa mno. Hivyo
Daudi akawaokoa wenyeji wa Keila. 6 Abiathari mwana wa Ahimeleki alipokuwa
amekimbilia kwa Daudi huko Keila, alibeba naivera mkononi mwake. 7 Sauli
aliambiwa kwamba Daudi amekwenda Keila. Sauli akasema, “Mungu amemweka
mkononi mwangu. Bila shaka amefungiwa ndani kwa sababu ameingia katika mji
ulio na malango na makomeo.” 8 Sauli akayaita majeshi yake yote kwa ajili ya vita,
waende hadi Keila, wamteke Daudi na watu wake. 9 Daudi alijua kwamba Sauli
alikuwa anapanga njama za kumdhuru yeye. Ndipo akamwambia kuhani Abiathari
kuhani, “Ulete hapa naivera.” 10 Kisha Daudi akasema, “BWANA, Mungu wa Israeli,
mtumishi wako hakika amesikia kwamba Sauli anatafuta namna ya kuja Keila, ili
auteketeze mji kwa ajili yangu. 11 Je, watu wa Keila watanisalimisha mkononi
mwake? Je, Sauli atashuka hadi huko, kama mtumishi wako alivyosikia? BWANA,
Mungu wa Israeli, nakusihi, tafadhali mwambie mtumishi wako. “BWANA akasema,
“Atakuja huko.” 12 Kisha Daudi akauliza, “Je, watu wa Keila watanisalimisha mimi na
watu wangu katika mkono wa Sauli?” BWANA akasema, “Watu hao watawasalimisha
kwao.” 13 Kisha Daudi na watu wake, waliokuwa kama mia sita, walitoka na
kwenda mbali na Keila, na wakazunguka kila sehemu. Kisha Sauli akaambiwa
kwamba Daudi ametoroka kutoka Keila, hivyo akasitisha kumfuatia. 14 Daudi alikaa
ngomeni katika jangwa, kwenye nchi ya milima katika jangwa la Zifu. Kila siku Sauli
alimtafuta, lakini Mungu hakumweka mkononi mwake. 15 Daudi aliona kwamba
Sauli amejitokeza kuangamiza maisha yake; basi Daudi alikuwa katika jjangwa
la Zifu huko Horeshi. 16 Kisha Yonathani, mwana wa Sauli, akaamuka akaenda
kwa Daudi huko Horshi, naye akamtia moyo amtumainie Mungu. 17 Akamwambia,
“Usiogope. Kwa maana mkono wa baba yangu Sauli hautakupata. Utakuwa mfalme
juu ya Israeli, na mimi nitakuwa msaidizi wako. Baba yangu Sauli pia anajua
hivyo.” 18 Basi wote wawili wakafanya agano mbele za BWANA. Kisha Daudi alibaki
Horeshi, na Yonathani akaenda nyumbani. 19 Nndipo Wazifi wakamwendea Sauli
huko Gibea wakisema, “Je, Daudi hakujificha kati yetu kwenye ngome huko Horeshi,
juu ya mlima wa Hakila, ulioko kusini mwa Yeshimoni? 20 Basi uje, mfalme!
Kulingana na matakwa yako, uje! Kazi yetu itakuwa kumtia katika mkono wa
mfalme.” 21 Sauli akasema, “Mbarikiwe na BWANA. Kwa sababu mmenihurumia.
22 Nendeni, mhakikishe sawasawa. Tafuteni na kujua maficho yake yako wapi na ni
nani amemwona huko. Nimeambiwa kwamba yeye ni mjanja sana. 23 Kwa hiyo
chunguzeni, mjue sehemu zote anakojificha. Baadaye rudini kwangu mkiwa na
taarifa kamili, na kisha nitaongozana nanyi. Ikiwa yupo katika nchi, nitamtafuta
kutoka miongoni mwa elfu zote za Yuda.” 24 Ndipo wakaamka na kwenda hadi
Zifu mbele ya Sauli. Wakati huo Daudi na watu wake walikuwa katika jangwa
la Maoni, huko Araba upande wa kusini mwa Yeshimoni. 25 Sauli na watu wake
wakaenda kumtafuta Daudi. Na Daudi akaambiwa habari hiyo, hivyo akateremka

hadi kwenye mlima wa miamba na akakaa katika jangwa la Maoni. Sauli aliposikia
hivyo, akamfukuza Daudi katika Jangwa la Maoni. 26 Sauli akaenda akawa upande
mmoja wa mlima, na Daudi na watu wake walikuwa wakienda upande mwingine wa
mlima. Daudi kwa haraka akatoweka akae mbali na Sauli. Kwa sababu Sauli na watu
wake walikuwa wakimzunguka Daudi na watu wake wawakamate, 27 mjumbe mmoja
akaja kwa Sauli na kusema, "Njoo, harakisha maana Wafilisti wamepanga uvamizi
juu ya nchi." 28 Kwa hiyo Sauli akarudi asimfuatie Daudi na akaenda kupambana
na Wafilisti. Kwa hiyo sehemu ile iliitwa Mwamba wa Maficho. 29 Daudi akapanda
kutoka huko na kukaa katika ngome ya Engedi.

# 24

1 Sauli aliporudi kuwafukuza Wafilisti, akaambiwa kwamba, "Daudi yuko katika
jangwa la Engedi." 2 Ndipo Sauli akachukua watu elfu tatu waliochaguliwa kutoka
Iraeli yote, wakaenda kumtafuta Daudi na watu wake katika miamba ya Mbuzi
Mwitu. 3 Akafika penye mazizi ya kondoo kando ya njia, mahali palipokuwa na pango.
Sauli akaingia ndani yake kujisaidia. Wakati huo Daudi na watu wake walikuwa
wamekaa mbali zaidi ndani ya pango lilelile. 4 Watu wake Daudi wakamwambia, "Hii
ndiyo siku ambayo BWANA aliisema akikuambia, 'Nitamweka adui wako mkononi
mwako, ili umtendee kama unavyotaka."' Kisha Daudi akainuka na kumnyemelea
kwa mbele kimya kimya na kulikata pindo la kanzu ya Sauli. 5 Baadaye moyo wa
Daudi ukamchoma kwa sababu alilikata pindo la kanzu ya Sauli. 6 Akawaambia
watu wake, "BWANA anisamehe, sikupaswa kumtendea jambo hili bwana wangu,
Mtiwa mafuta wa BWANA, kwa kunyoosha mkono wangu juu yake, maana yeye
ni masihi wa BWANA." 7 Hivyo Daudi akawakemea watu wake kwa maneno haya,
na kuwazuia wasimpige Sauli. Sauli akasimama, akatoka pangoni, na kwenda
zake. 8 Baadaye tena, Daudi akasimama juu, akatoka pangoni, na kumwita Sauli:
"Bwana wangu mfalme." Sauli alipotazama nyuma, Daudi akasujudu hadi chini
na kuonyesha heshima. 9 Daudi akamwambia Sauli, "Kwa nini unawasikiliza watu
ambao wanasema, "Angalia, Daudi anatafuta kukudhuru?' 10 Leo macho yako
yameona jinsi BWANA alivyokuweka mkononi mwangu tulipokuwa ndani ya pango.
Wengine waliniambia nikuuwe, lakini nilikuacha hai. Nikasema, 'Sitanyoosha mkono
wangu juu ya bwana wangu; kwa kuwa ni masihi wa BWANA.' 11 Tazama, baba
yangu, angalia pindo la kanzu yako mkononi mwangu. Kwa maana kama nilikata
pindo la kanzu yako na sikukuua, basi ujuwe na uone kwamba sina uovu au kosa
katika mkono wangu, na sijafanya dhambi juu yako, ingawa unawinda kuutoa uhai
wangu. 12 BWANA aamue kati yangu na wewe, na BWANA anilipizie kisasi juu
yako, lakini mkono wangu kamwe hautakuwa juu yako. 13 Kama mithali ya wazee
isemavyo, 'Katika waovu hutoka uovu.' Lakini mkono wangu hautakuwa juu yako.
14 Mfalme wa Israeli ametoka kumuandama nani? Unamsaka nani? Unasaka mzoga
wa mbwa! Unasaka kiroboto! 15 BWANA na awe mwamuzi na atoe hukumu kati
yangu na wewe, na akaione, na akatetee sababu yangu na aniruhusu kuepuka mkono
wako." 16 Daudi alipomaliza kuongea maneno haya kwa Sauli, Sauli akasema, "Hii ni
sauti yako, mwanangu Daudi?" Sauli alinyanyua sauti yake akalia. 17 Akamwambia
Daudi, "Wewe ni mwenye haki kuliko mimi. Kwa sababu umenilipa mazuri, wakati
mimi nimekulipa maovu. 18 Leo umetangaza jinsi ulivyonitendea mazuri, kwa
sababu hukuniua wakati BWANA aliponiweka katika rehema yako. 19 Kwa kuwa
mtu akimpata adui yake, atamwacha aende zake salama? Na BWANA akuzawadie
mema kwa kile ulichonifanyia leo. 20 Basi, najua kwa hakika kwamba utakuwa
mfalme na kwamba ufalme wa Israeli utaimarika katika mkono wako. 21 Niapie
kwa BWANA kwamba baada yangu hautawakatilia mbali uzao wangu, na kwamba

hautaliharibu jina langu katika nyumba ya baba yangu.” 22 Hivyo Daudi akamwapia
Sauli kiapo. Kisha Sauli akaenda nyumbani, lakini Daudi na watu wake wakapanda
kwenda ngomeni.

# 25

1 Basi Samweli akafariki. Waisraeli wote wakakusanyika pamoja na kumwom-
boleza, na wakamzika nyumbani kwake huko Rama. Kisha Daudi akainuka na
akashuka hadi jangwa la Parani. 2 Kulikuwa na mtu mmoja huko Maoni, na mali
zake zilikuwa huko Karmali. Mtu huyo alikuwa tajiri sana. Alikuwa na kondoo
elfu tatu na mbuzi elfu moja. Naye alikuwa akiwakata manyoya kondoo wake
huko Karmeli. 3 Na mtu huyo aliitwa Nabali, na jina la mke wake aliitwa Abigaili.
Mwanamke huyo alikuwa mwenye busara na mzuri kwa sura. Lakini mwanaume
alikwa mkaidi na mwovu katika mambo yake. Alikuwa wa uzao wa nyumba
ya Kalebu. 4 Daudi akasikia akiwa jangwani kwamba Nabali alikuwa akiwakata
manyoya kondoo wake. 5 Hivyo Daudi aliwatuma kwake vijana kumi. Akawaambia
wale vijana, “Pandeni kwanda Karmeli, mwendeeni Nabali, na mkamsalimie kwa
jina langu. 6 Mtamwambia, 'Uishi katika baraka, Uwe na amani na nyumba yako
iwe na amani, na wote ulionao wawe na amani. 7 Nasikia kwamba unao wakata
manyoya. Wachungaji wako walikuwa pamoja nasi, na hatukuwafanyia ubaya, na
muda wote wakiwa Karmeli hawakupotelewa kitu chochote. 8 Waulize vijana wako,
nao watakuambia. Basi vijana wangu wapate kibali machoni pako, maana tumefika
siku ya sherehe. Tafadhali utoe cho chote ulicho nacho mkononi kwa watumishi wako
na kwa Daudi mwanao.'” 9 Vijana wa Daudi walipofika, walimwambia Nabali yote
haya kwa niaba ya Daudi na kisha wakasubiri. 10 Nabali akawajibu watumishi wa
Daudi, “Daudi ni nani? Na ni nani mwana wa Yese? Siku hizi wapo watumishi wengi
wanaotoroka bwana zao. 11 Je, nichukue mkate wangu na maji yangu na nyama
yangu ambayo nimewachinjia wakata manyoya wangu, na niwape watu wanaotoka
nisikokujua?” 12 Hivyo vijana wa Daudi waligeuka na kurudi, nakumwambia kila
kitu kilichosemwa. 13 Daudi akawaambia watu wake, “Kila mtu ajifunge upanga
wake.” Kila mtu akajifunga upanga wake. Daudi naye pia akajifunga upanga
wake. Yapata kama watu mia nne wakafuatana na Daudi, na wengine mia mbili
walibaki kulinda mizigo yao. 14 Lakini kijana mmojawapo alimwambia Abigaili, mke
wa Nabali akasema, “Daudi aliwatuma wajumbe kutoka jangwani waje wamsalimu
bwana wetu, na yeye akawatukana. 15 Bado watu hawa walitutendea mema.
Hatukudhurika na hatukupoteza chochote wakati wote tulipotembea nao tulipokuwa
mbugani. 16 Walikuwa ukuta wetu usiku na mchana, wakati wote tulikuwa pamoja
nao tukichunga kondoo. 17 Kwa hiyo tambua hili na zingatia utafanya nini, maana
ubaya unamvizia bwana wetu, na utakuwa juu ya nyumba yake yote. Yeye ni mtu
asiyefaa na hakuna awezaye kushauriana naye.” 18 Ndipo Abigaili akaharakisha na
akachukuwa mikate mia mbili, chupa mbili za divai, kondoo watano waliokwisha
andaliwa, vipimo vitano vya bisi, vishada mia moja vya zabibu, na mikate mia
mbili ya tini na akavipakia juu ya punda. 19 Akamwambia kijana wake, “Tangulia
mbele yangu, nami nitakuja nyuma yako.” Lakini hakumwambia mmewe Nabali.
20 Alipokuwa akienda juu ya punda wake na kutelemka penye kificho cha mlima,
Daudi na watu wake walishuka chini wakimwelekea Abigaili, naye akakutana nao.
21 Basi Daudi alikuwa amesema, “Hakika nimelinda bure vyote alivyonavyo mtu
huyu huko nyikani, na vyote alivyonavyo hakuna kilichopotea, pamoja na hayo
amenilipa mabaya badala ya mema. 22 Mungu na anitendee hivyo mimi, Daudi, pia
iwe zaidi, iwapo nitamwacha hata mtu mmoja wa kwake akiwa hai ifikapo kesho
asubuhi. 23 Abigaili alipomwona Daudi, aliharakisha na kushuka chini ya punda

wake, akalala kifudifudi na kujiinamisha hadi chini. 24 Akamwangukia miguuni
pake na kusema, “Juu yangu tu, bwana wangu, na uwe uovu. Tafadhali acha
mjakazi wako aseme nawe, tena uyasikilize maneno ya mjakazi wako. 25 Nakusihi
bwana wangu usimjali mtu huyu asiyefaa, Nabali, kwa maana kama jina lake lilivyo,
ndivyo alivyo. Jina lake ni Nabali, na upumbavu uko pamoja naye. Lakini mimi
mjakazi wako sikuwaona vijana wa bwana wangu, uliowatuma. 26 Sasa basi, bwana
wangu, kama BWANA aishivyo, na kama unavyoishi, kwa kuwa BWANA amekuondoa
kutoka kumwaga damu, na kuacha kulipiza kisasi kwa mkono mwenyewe, basi
adui zako, na wale ambao wanatafuta kumfanyia uovu bwana wangu, wawe kama
Nabali 27 Na sasa zawadi hii ambayo mjakazi wako ameileta kwa bwana wangu,
na wapewe vijana ambao wanamfuata bwana wangu. 28 Tafadhali ulisamehe kosa
la mjakazi wako, maana BWANA hakika atamfanyia bwana wangu nyumba imara,
kwa sababu bwana wangu anapigana vita vya BWANA; na uovu hautaonekana
ndani yako maadamu unaishi. 29 Na ingawa watu wangeinuka na kukuandama
ili wakuue, bado uhai wa bwana wangu utafungwa katika furushi la walio hai
na BWANA Mungu wako; na atayatupa maisha ya adui zako mbali, kama vile
kutoka katika mfuko wa kombeo. 30 Na itakuwa, BWANA atakapokuwa amemtimizia
bwana wangu mambo yote mazuri ambayo amekuahidi, na alivyokufanya kiongozi
juu ya Israeli, 31 jambo hili halitakuwa huzuni kwako, wala chukizo moyoni kwa
bwana wangu, kwa sababu hukumwaga damu bila sababu, na hujajilipizia kisasi.
Na BWANA akikuletea mafanikio, umkumbuke mjakazi wako.” 32 Ndipo Daudi
akamwambia Abigaili, “BWANA, Mungu wa Israeli, abarikiwe, aliyekutuma uonane
na mimi leo. 33 Na hekima yako ibarikiwe, nawe umebarikiwa, kwa sababu leo
umenizuia nisiwe na hatia ya kumwaga damu, na kutojilipizia kisasi kwa mkono
wangu mwenyewe. 34 Kwa kweli, kama BWANA, Mungu wa Israeli, aishivyo,
ambaye amenizuia nisikuumize, kama usinge harakisha kuja ukutane nami, kwa
hakika kesho asubuhi asinge salia hata mtoto mmoja wa kiume kwa Nabali.”
35 Kwa hiyo Daudi akavipokea kutoka mkononi mwake vile alivyokuwa amemletea;
akamwambia, “Nenda kwa amani hadi nyumbani kwako; tazama, nimeisikiliza sauti
yako na nimekubali.” 36 Abigaili akarudi kwa Nabali; tazama, alikuwa akifanya
sherehe katika mji wake, kama sherehe ya mfalme; na moyo wa Nabali ulifurahi
ndani yake, kwa sababu alikwa amelewa sana. Kwa hiyo hakumwambia chochote
kabisa hadi kulipopambazuka 37 Ikawa asubuhi, divai ilipokuwa imemtoka Nabali,
basi mkewe akamwambia mambo hayo; moyo wake ukafa ndani yake, na akawa
kama jiwe. 38 Ikawa baada ya siku kumi BWANA alimpiga Nabali naye akafa.
39 Naye Daudi aliposikia kwamba Nabali amekufa, akasema, “BWANA abarikiwe,
aliyenichukulia hatua ya shutuma yangu kutoka mkono wa Nabali, na kumzuia
mtumishi wake asifanye maovu. Na amemrudishia Nabali tendo la uovu juu ya
kichwa chake mwenyewe.” Ndipo Daudi akawatuma watu wakaongee na Abigaili, ili
amchukue awe mke wake. 40 Watumishi wake Daudi walipofika kwa Abigaili huko
Karmeli, wakaongea naye na kusema, “Daudi ametutuma kwako tukuchukue hadi
kwake uwe mke wake.” 41 Abigaili aliinuka, akainamisha uso chini, na akasema,
“Tazama, mjakazi wako ni mtumwa aoshaye miguu ya watumishi wa bwana wangu.”
42 Akaharakisha na kuamka, akapanda punda akiwa na vijakazi wake watano
waliofuatana naye; akawafuata wajumbe wa Daudi, na akawa mke wake. 43 Daudi
pia alimchukua Ahinoamu wa Yezreeli akamwoa; wote wawili wakawa wake zake.
44 Wakati huo Sauli alikuwa amempa Palti, mwana wa Laishi mtu wa Galimu, Mikali,
binti yake, aliyekuwa mke wa Daudi.

# 26

[1] Wazifi wakamwendea Sauli huko Gibea na kusema, “Je, Daudi akujificha katika
vilima vya Hakila, ambavyo viko mbele ya jangwa?” [2] Kisha Sauli akaamka na
kwenda chini ya jangwa la Zifu, akiwa na watu elfu tatu waliochaguliwa katika
Israeli, wamtafute Daudi katika jangwa la Zifu. [3] Sauli akaweka kambi kwenye
kilima cha Hakila, kilicho mbele ya jangwa, kando ya barabara. Lakini Daudi alikuwa
akikaa nyikani, na akaona kwamba Sauli alikuwa anamfuatia huko jangwani. [4] Hivyo
Daudi akawatuma wapelelezi na akafahamu kwamba hakika Sauli alikuwa amekuja.
[5] Daudi akaamka na kwenda hadi mahali ambapo Sauli alipiga kambi; akaona mahali
alipolala Sauli, na Abneri mwana wa Neri, mkuu wa jeshi lake; Sauli alilala katikati
ya kambi, na watu walipiga kambi kumzunguka, na wote wamesinzia. [6] Ndipo
Daudi akamwambia Ahimeleki Mhiti, na Abishai mwana wa Seruya, ndugu yake
Yoabu, “Ni nani atakwenda nami kambini kwa Sauli? Abishai akasema, “Mimi
nitashuka pamoja nawe.” [7] Hivyo Daudi na Abishai wakaliendea jeshi usiku. Na
Sauli alikuwapo akisinzia ndani ya kambi, mkuki wake umechomekwa chini pembeni
mwa kichwa chake. Abneri na Askari wake wamelala kwa kumzunguka. [8] Kisha
Abishai akamwambia Daudi, “Leo Mungu amemweka adui yako mkononi mwako.
Basi tafadhali acha nimchome mkuki nimtoboe hadi chini kwa pigo moja. Sitampiga
mara mbili.” [9] Daudi akamwambia Abishai, “Usimwangamize; kwa maana nani
awezaye kunyoosha mkono wake dhidi ya mtiwa mafuta wa BWANA na asiwe na
hatia?” [10] Daudi akasema, “Kama BWANA aishivyo, BWANA atamuua, au siku ya
kufa kwake itakuja, au atakwenda katika vita na ataangamia. [11] BWANA apishe mbali
nisinyooshe mkono wangu dhidi ya mtiwa mafuta wake; lakini sasa, nakusihi chukua
mkuki uliokichwani pake na jagi la maji, tuondoke.” [12] Hivyo Daudi akachukua mkuki
na jagi la maji kutoka kichwani pa Daudi, wakatoweka. Hakuna mtu aliyewaona
au kufahamu habari hii, wala hakuna aliyetoka usingizini, maana wote walisinzia,
kwa sababu usingizi mzito kutoka kwa BWANA uliwaangukia. [13] Kisha Daudi
akaenda upande mwingine na akasimama juu ya mlima mbali sana; ukiwepo umbali
mkubwa katikati yao. [14] Daudi akawapigia kelele watu hao na Abneri mwana
Neri; akisema, “Hujibu neno, Abneri?” Ndipo Abneri akajibu na kusema, “Wewe
ni nani unayempigia mfalme kelele?” [15] Daudi akamwambia Abneri, “Wewe siye
mtu jasiri? Ni nani yuko kama wewe katika Israeli? Kwa nini basi hukukaa
macho kumlinda bwana wako mfalme? Kwa maana mtu fulani aliingia kumuua
mfalme, bwana wako. [16] Jambo hili ulilolifanya siyo zuri. Kama BWANA aishivyo,
unapaswa kufa kwa sababu hukumlinda bwana wako, mtiwa mafuta wa BWANA.
Na sasa tazama ulipo mkuki wa mfalme, na jagi la maji lililokuwa kichwani pake.”
[17] Sauli aliitambua sauti ya Daudi akasema, “Hiyo ni sauti yako, Daudi mwanangu?”
Daudi akasema, “Ni sauti yangu, mfalme, bwana wangu.” [18] Daudi akasema, “Kwa
nini bwana wangu anamwandama mtumishi wake? Nimefanya nini? Mkononi
mwangu kuna uovu gani? [19] Kwa hiyo sasa, nakusihi, bwana wangu mfalme asikilize
maneno ya mtumishi wake. Kama ni BWANA ndiye amekuchochea dhidi yangu,
na aikubali sadaka; lakini kama ni wanadamu, na walaaniwe mbele za BWANA,
maana leo wamenifukuza, nisishikamane na urithi wa BWANA; wameniambia,
'Nenda ukaabudu miungu mingine.' [20] Kwa hiyo, sasa, usiiachilie damu yangu
ianguke ardhini mbali na uwepo wa BWANA; kwa kuwa mfalme wa Israeli ametoka
nje kutafuta kiroboto, kama vile mtu awindavyo kware milimani.” [21] Kisha Sauli
akasema, “Nimefanya dhambi. Rudi, Mwanangu, Daudi; maana sitakudhuru tena,
kwa sababu leo maisha yangu yalikuwa yenye thamani machoni pako. Tazama,
nimetenda upumbavu na nimekosa sana.” [22] Daudi akajibu na akasema, “Tazama,
mkuki wako uko hapa, mfalme! Mruhusu kijana mmojawapo aje auchukue na aulete

kwako. 23 Na BWANA amlipe kila mtu kwa ajili ya uadilifu wake na kwa uaminifu
wake; kwa sababu leo BWANA alikuweka mkononi mwangu, lakini nisinge mpiga
mtiwa mafuta wake. 24 Na tazama, kama maisha yako leo yalivyokuwa ya thamani
machoni pangu, vivyo hivyo maisha yangu yathaminiwe sana machoni pa BWANA,
na aweze kuniokoa katika shida zote." 25 Ndipo Sauli akamwambia Daudi, "Na
ubarikiwe, mwanangu Daudi, ili uweze kutenda mambo makuu, na hakika uweze
kufanikiwa." Ndipo Daudi akaenda zake, na Sauli akarudi kwake.

# 27

1 Daudi alisema moyoni mwake, "Basi, siku moja nitaangamia kwa mkono wa Sauli;
hakuna jambo zuri kwangu kuliko kutoroka hadi nchi ya Wafilisti; Sauli atakata
tamaa asinitafute tena ndani ya mipaka yote ya Israeli; kwa njia hii nitaponyoka
kutoka mkono wake." 2 Daudi akaondoka na kuvuka, akiwa pamoja na watu mia sita
hadi kwa Akishi mwana wa Maoki, mfalme wa Gathi. 3 Daudi akaishi na Akishi huko
Gathi pamoja na watu wake, na kila mtu na familia yake, na Daudi akiwa na wake
zake wawili, Ahinoamu Myezreeli, na Abigaili Mkarmeli aliyekuwa mke wa Nabali.
4 Sauli akaambiwa kuwa Daudi amekimbilia Gathi, hivyo hakumtafuta tena. 5 Daudi
akamwambia Akishi, "Kama nimepata kibali machoni pako, wanipatie mahali katika
mojawapo ya miji ya nchi, ili nikae huko: kwa nini mtumishi wako akae pamoja
na wewe katika mji wa kifalme?" 6 Hivyo siku hiyo Akishi akampa Daudi Ziklagi;
ndiyo sababu mji wa Ziklagi ni mali ya wafalme wa Yuda hadi leo. 7 Idadi ya siku
ambazo Daudi aliishi katika nchi ya Wafilisti ulikuwa mwaka mmoja na miezi minne.
8 Daudi na watu wake walizipiga sehemu mbalimbali, wakiteka nyara Wageshuri,
Wagirizi, na Waamaleki; kwa maana mataifa hayo ndio walikuwa wakaaji wa nchi,
kwa uelekeo wa kwenda Shuri hadi kufika nchi ya Misri. Walikuwa wamekaa katika
nchi hiyo toka nyakati za zamani. 9 Daudi aliipiga nchi na hakumwacha mwanaume
wala mwanamke akiwa hai; akatwaa kondoo, ng'ombe, punda, ngamia, na nguo;
kisha alirudi na kufika tena kwa Akishi. 10 Ndipo Akishi humuuliza, "Je, leo umefanya
mashambulizi dhidi ya nani?" Daudi humjibu, "Nimefanya dhidi ya kusini mwa
Yuda," au dhidi ya kusini mwa Wayerameeli," au "dhidi ya kusini mwa Wakeni."
11 Daudi asingemwacha mwanaume wala mwanamke akiwa hai awalete hadi Gathi,
akisema, "ili wasije kututeta, 'Daudi amefanya hivi na vile."' Hivi ndivyo alivyofanya
kwa kipindi chote alichokaa katika nchi ya Wafilisti. 12 Akishi alimwamini Daudi,
akisema, "Amesababisha watu wake Israeli wamchukie kabisa; kwa hiyo atakuwa
mtumishi wangu milele."

# 28

1 Ikawa katika siku hizo Wafilisti walikusanya majeshi yao pamoja kwa ajili ya vita,
wapigane na Israeli. Akishi akamwambia Daudi, "Ujue kwa hakika kwamba utak-
wenda nami ndani ya jeshi, wewe na watu wako." 2 Naye Daudi akamwambia Akishi,
"Sasa utajua kile ambacho mtumishi wako anaweza kufanya." Akishi akamwambia
Daudi, "Basi sasa, nitakufanya uwe mlinzi wangu binafsi daima." 3 Samweli alikuwa
amefariki; Waisraeli wote walimwomboleza na kumzika huko Rama, katika mji
wake mwenyewe. Wakati huo Sauli alikuwa amewafukuza kutoka nchini wote
walioongea na wafu au pepo. 4 Wafilisti walijikusanya wao wenyewe wakaja na
kuweka kambi huko Shunemu; na Sauli akawakusanya Israeli wote pamoja, na
wakaweka kambi yao huko Gilboa. 5 Sauli alipoona jeshi la Wafilisti, aliogopa na
moyo wake ukatetemeka sana. 6 Sauli alipomuomba BWANA kwa ajili ya msaada,
BWANA hakumjibu - si kwa ndoto wala kwa Urimu, wala kwa manabii. 7 Ndipo Sauli
akawaambia watumishi wake, "Mnitafutie mwanamke ambaye anaweza kuongea na

wafu, ili ni mwendee na kutafuta msaada wake.” Watumishi wake wakamwambia,
“Tazama, yupo mwanamke huko Endori awezaye kuongea na wafu.” 8 Basi Sauli
akajigeuza, akavaa nguo nyingine tofauti, akaondoka yeye pamoja na watu wawili;
wakamwendea yule mwanamke wakati wa usiku. Akasema, “Nitabirie, nakuomba,
kwa kuongea na wafu, na uniinulie yule nitakayekutajia.” 9 Yule mwanamke
akamwambia, “Tazama, unajua alichofanya Sauli, jinsi alivyowafukuza kutoka katika
nchi wanaoongea na wafu au mizimu. Basi kwa nini mnatega mtego kwa ajili
ya uhai wangu, ili kuniua?” 10 Sauli akamwapia kwa BWANA na kusema, “Kama
BWANA aishivyo, hakuna adhabu utakayopata kutokana na jambo hili.” 11 Kisha
yule mwanamke akasema, “Je, nikuinulie nani?” Sauli akasema, “Niinulie Samweli.”
12 Yule mwanamke alipomwona Samweli, akalia kwa sauti kuu na kusema na
Sauli, akisema, “Kwa nini umenidanganya? Maana wewe ni Sauli.” 13 Mfalme
akamwambia, “Usiogope. Unaona kitu gani?” Yule mwanamke akamwambia Sauli,
“Naona mungu akitoka katika nchi.” Akamuuliza mwanamke, 14 “Je, anafanana
na nani?” Mwanamke akajibu, “Mtu mzee anazuka; naye amevaa kanzu.” Sauli
akafahamu kuwa huyo ni Samweli, naye Sauli akainamisha uso wake hadi chini
akionesha heshima. 15 Samweli akamwambia Sauli, “Kwa nini umenisumbua na
kuniinua juu?” Sauli akajibu, “Nimetaabika sana, maana Wafilisti wamepanga vita
dhidi yangu, na Mungu ameniacha na hanipi majibu tena, si kwa manabii, wala
kwa ndoto. Kwa hiyo nimekuita, ili unijulishe kile nitakachofanya.” 16 Samweli
akasema, “Kwa kuwa BWANA amekuacha, basi unaniuliza nini, naye amekuwa
adui yako? 17 BWANA amekutendea kile alichosema kuwa angekifanya. BWANA
amerarua ufalme kutoka mkononi mwako na amempa ufalme mtu mwingine -
amempa Daudi. 18 Kwa sababu hukuitii sauti ya BWANA na hukutekeleza hasira
yake kali juu ya Amaleki, kwa hiyo leo naye amefanya hili kwako. 19 Zaidi ya
hayo, BWANA atamweka Israeli pamoja na wewe katika mkono wa Wafilisti. Kesho
wewe na wanao mtakuwa pamoja nami. BWANA pia ataliweka jeshi la Israeli
katika mkono wa Wafilisti.” 20 Ndipo ghafla Sauli alianguka chini kifudifudi na
aliogopa kwa sababu ya yale maneno ya Samweli. Aliishiwa nguvu mwilini mwake,
kwa kuwa siku hiyo alikuwa hajala chakula, hata kwa usiku huo wote. 21 Ndipo
yule mwanamke akaja kwa Sauli na akaona kwamba Sauli amepata shida, naye
akamwambia, “Tazama, mjakazi wako ameisikiliza sauti yako; Nimeyaweka maisha
yangu mkononi mwangu na nimeyasikiliza maneno uliyoniambia. 22 Hivyo basi,
nakusihi, sikiliza pia sauti ya mjakazi wako, na uniruhusu nilete chakula kidogo
mbele yako. Ule ili upate nguvu za kwenda kule uendako.” 23 Lakini Sauli
alikataa na kusema, “Sitakula.” Lakini watumishi wake, pamoja na yule mwanamke,
wakamlazimisha hatimaye alisikiliza sauti zao. Hivyo aliinuka kutoka chini na kukaa
kitandani. 24 Yule mwanamke alikuwa na ndama mnono hapo nyumbani; akafanya
haraka na kumchinja; akachua unga, akaukanda, na akatengeneza mikate isiyotiwa
chachu kwa unga huo. 25 Akaileta mbele ya Sauli na watumishi wake, nao wakala.
Baaadaye waliinuka na kuondoka usiku huo.

# 29

1 Basi Wafilisti walikusanya pamoja majeshi yao yote huko Afeki; Waisraeli
wakapiga kambi karibu na chemchemi iliyoko Yezreeli. 2 Nao wakuu wa Wafilisti
wakapitwa na mamia kwa maelfu; Daudi na watu wake wakapita wakiwa wa
mwisho pamoja na Akishi. 3 Kisha wakuu wa Wafilisti wakasema, “Hawa Waebrania
wanafanya nini hapa?” Akishi akawaambia wakuu wengine wa Wafilisti, “Huyu si
Daudi, mtumishi wa Sauli, mfalme wa Israeli, ambaye amekaa nami kwa siku hizi, au
kwa miaka hii, nami nimeona hana kosa tangu aje kwangu hadi leo?” 4 Lakini wale

wakuu wa Wafilisti walimkasirikia Akishi; wakamwabia, Mfukuze mtu huyo, aende
kwake kule ulikompatia; usimruhusu aende nasi vitani, ili asiwe adui yetu katika
vita. Kwa jinsi gani mtu huyu angeweza kufanya amani na bwana wake? Siyo kwa
gharama ya vichwa vya watu wetu? 5 Je, huyu siye Daudi ambaye walimuimba kwa
kupokezana na kucheza, wakisema: 'Sauli ameua maelfu yake, Na Daudi makumi
elfu yake?"' 6 Ndipo Akishi alimwita Daudi na kumwambia, "Kama BWANA aishivyo,
umekuwa mwema, na kutoka kwako na kuingia kwako pamoja nami katika jeshi
ni kwema kama nionavyo mimi; maana sijaona kosa kwako tangu siku unakuja
kwangu hadi siku hii ya leo. Hata hivyo, wakuu hawakupendi. 7 Basi sasa rudi na
uende kwa amani, ili usiwakwaze wakuu wa Wafilisti." 8 Daudi akamwambia Akishi,
"Lakini nimefanya nini? Kitu gani umekiona kwa mtumishi wako kwa muda ambao
nimekuwa mbele yako hadi leo, kiasi kwamba nisiende kupigana na adui za bwana
wangu mfalme?" 9 Akishi akajibu na kumwambia Daudi, "Najua kwamba hauna
lawama mbele zangu kama alivyo malaika wa Mungu; hata hivyo, wale wakuu wa
Wafilisti wamesema, Kamwe hatapanda pamoja nasi hadi vitani.' 10 Basi sasa amka
asubuhi na mapema na watumishi wa bwana wako waliokuja pamoja nawe; mara
tu muamkapo asubuhi na mapema na kupata mwanga, ondokeni." 11 Hivyo Daudi
aliamka mapema, yeye pamoja na watu wake, waondoke asubuhi, warudi kule katika
nchi ya Wafilisti. Lakini Wafilisti walipanda kwenda Yezreeli.

# 30

1 Ikawa, Daudi na watu wake walipokuwa wamefika Ziklagi siku ya tatu, Waamaleki
walifanya mashambulizi katika Negevu na Ziklagi. Waliupiga Ziklagi, wakauchoma
moto mji, 2 na kuwachukua mateka wanawake na kila mmoja aliyekuwa ndani
yake, mkubwa kwa mdogo. Wao hawakuua hata mmoja, lakini waliwachukua
watu na kuondoka nao. 3 Daudi na watu wake walipofika kwenye mji, ulikuwa
umechomwa moto - na wake zao, watoto wao wakiume na wakike walichukuliwa
mateka. 4 Ndipo Daudi na watu aliokuwa nao wakapaza sauti zao na kulia hadi
walipokuwa hawana nguvu zaidi za kulia. 5 Wake wawili wa Daudi walichukuliwa
mateka, yaani Ahinoamu Myezreeli, na Abigaili aliyekuwa mke wa Nabali Mkarmeli.
6 Daudi aliguswa sana, maana watu walikuwa wanaongea kuhusu kumpiga mawe,
kwa sababu roho za watu wote walihuzunika, kila mtu kwa ajili ya mtoto wake
wakiume na wakike, lakini Daudi alijiimarisha katika BWANA, Mungu wake. 7 Daudi
akamwambia Abiathari, kuhani, mwana wa Ahimeleki, "Tafadhali, niletee hapa ile
naivera."Abiathari akaileta hiyo naivera kwa Daudi. 8 Daudi akamwomba BWANA
kwa ajili ya mwongozo, akisema, "Je, kama nikiliandama jeshi hili, nitalipata?"
BWANA akamjibu, "Wafuate, maana kweli utawapata, na kwa hakika utarudisha kila
kitu." 9 Kwa hiyo Daudi akaenda, yeye na wale watu mia sita waliokuwa pamoja
naye; nao wakafika katika kijito cha Bethori, mahali walipokaa wale walioachwa
nyuma. 10 Lakini Daudi aliendelea kuwafuata, yeye na watu mia nne; maana
wale mia mbili walibaki nyuma, wakiwa wamechoka kiasi cha kutoweza kuvuka
kijito cha Besori. 11 Nao walimkuta Mmisri shambani na wakamleta kwa Daudi;
wakampatia mkate, na akala; wakampa maji ya kunywa; 12 kisha walimpa kipande
cha keki ya tini na vishada viwili vya zabibu. Alipomaliza kula, akapata nguvu
tena, kwa kuwa alikuwa hajala mkate wala kunywa maji, siku tatu mchana na
usiku. 13 Ndipo Daudi akamuuliza, "Wewe ni mtu wa nani? Je, unatoka wapi?"
Naye akajibu, "Mimi ni kijana wa Misri, mtumishi wa Mwamaleki mmoja; bwana
wangu aliniacha, kwa sababu siku tatu zilizopita nilikuwa mgonjwa. 14 Tulifanya
mashambulizi dhidi ya Negevu ya Wakerethi, na iliyochini ya Yuda, na ile Negevu
ya Kalebu, na kuichoma moto Ziklagi." 15 Daudi akamwambia, "Je, utanipeleka hadi

kwa jeshi lililofanya mashabulizi?" Huyo Mmisri akasema, "Uniapie kwa Mungu
kwamba hautaniua au kunisaliti na kuniweka katika mikono ya bwana wangu, nami
nitakupeleka liliko hilo jeshi." 16 Yule Mmisri alipompeleka huko Daudi, hao wateka
nyara walikuwa wametawanyika kila sehemu, wakila na kunywa, na wakicheza, kwa
sababu ya nyara zote walizokuwa wamezitwaa kutoka nchi ya Wafilisti na kutoka
nchi ya Yuda. 17 Daudi akawashambulia tangu jua lilipozama hadi jioni ya siku ya
pili. Hakuna mtu aliyeponyoka isipokuwa vijana mia nne, waliopanda ngamia na
kukimbia. 18 Daudi akarudisha vyote ambavyo Waamaleki walikuwa wamevichukua;
na Daudi akawaokoa wake zake wawili. 19 Hakuna kilichopotea, si kidogo wala
kikubwa, si watoto wa kiume wala wa kike, si mali iliyotekwa, wala chochote
ambacho wavamizi alikichukuwa kwa ajili yao. Daudi akawa amerejesha kila kitu.
20 Akachukua makundi yote ya kondoo na ng'ombe, ambayo watu waliyatanguliza
mbele ya ng'ombe wengine. Wakisema, "Hizi ni nyara za Daudi." 21 Daudi akafika
kwa wale watu mia mbili waliokuwa wamechoka kufuatana naye, wale walioachwa
wakae katika kijito cha Besori. Watu hawa wakajitokeza kumlaki na watu waliokuwa
naye. 22 Ndipo watu wote waovu na wasiofaa miongoni mwa waliokwenda na Daudi
wakasema, "Kwa sababu watu hawa hawakwenda nasi, hatutawapa chochote kutoka
katika nyara tulizorudisha. Isipokuwa kila mtu aweza kuchukuwa mke na watoto
wake, wawatoe na kwenda zao." 23 Ndipo Daudi akasema, "Ndugu zangu, msifanye
hivyo, kwa vitu ambavyo BWANA ametupatia. Ametuhifadhi na kuwaweka mkononi
mwetu wavamizi waliotuinukia. 24 Ni nani atawasikiliza kuhusu jambo hili? Kwa
maana mgawo ni kwa yeyote aendae vitani, basi pia mgawo ni kwa yeyote aliyelinda
mizigo; Nao watapata tena kilicho sawa." 25 Ilikuwa hivyo tangu siku hiyo hadi leo,
maana Daudi aliamua iwe sheria na amri kwa Israeli. 26 Daudi alipofika Ziklagi,
alituma sehemu ya nyara kwa wazee wa Yuda, kwa rafiki zake, akisema, "Tazama,
hii ni zawadi yenu kutokana na nyara za adui wa BWANA." 27 Zawadi zilienda kwa
wazee waliokuwa Bethueli, na kwa hao waliokuwa Ramothi iliyoko kusini, na kwa
hao waliokuwa Yatiri, 28 na kwa hao waliokuwa Aroeri, na kwa hao waliokuwa
Sifmothi, na kwa hao waliokuwa Eshtemoa 29 Pia kwa wazee waliokuwa Rakali, na
kwa hao waliokuwa katika miji ya Wayerameeli, na kwa hao waliokuwa katika miji
ya Wakeni, 30 na kwa hao waliokuwa Horma, na kwa hao waliokuwa Borashani, na
kwa hao waliokuwa Athaki, 31 na kwa hao waliokuwa Hebroni, na kwa sehemu zote
ambazo Daudi mwenyewe na watu wake walizoea kwenda.

# 31

1 Basi Wafilisti wakapigana dhidi ya Waisraeli. Waisraeli wakakimbia mbele
ya Wafilisti na wakaanguka chini wakafa katika mlima wa Gilboa. 2 Wafilisti
wakamwandama Sauli na wanawe kwa karibu. Wakawaua wanawe Yonathani,
Abinadabu, and Malkishua. 3 Vita vikamwelemea Sauli, na wapiga upinde wakam-
pata. Akapata maumivu makali kwa sababu yao. 4 Kisha Sauli akamwambia mbeba
silaha wake, "Chomoa upanga wako unichome nao. Vinginevyo, hawa wasiotahiriwa
watakuja na kuninyanyasa." Lakini mbeba silaha wake hakukubali, kwa kuwa
aliogopa sana. Hivyo Sauli alichukua upanga wake mwenyewe na kuuangukia. 5 Yule
mbeba silaha akaona kwamba Sauli amekufa, yeye naye vivyo hivyo akauangukia
upanga wake akafa pamoja naye. 6 Kwa hiyo Sauli alikufa, wanawe watatu, na mbeba
silaha wake - watu hawa wote walikufa pamoja siku iyo hiyo. 7 Watu wa Israeli
waliokuwa upande mwingine wa bonde, na hao waliokuwa ng'ambo ya Yordani,
walipoona kwamba Waisraeli wamekimbia, na kwamba Sauli na wanawe wamekufa,
waliiacha miji yao na kukimbia, nao Wafilisti wakaja na kukaa humo. 8 IKawa katika
siku iliyofuata, Wafilisti wakafika kuchukua nyara za waliokufa, ndipo wakamuona

Sauli na wanawe watatu wameanguka juu ya mlima wa Gilboa. 9 Nao wakakata
kichwa chake na kuondoa silaha zake, na wakawatuma wajumbe kwenda pande zote
katika nchi ya Wafilisti kutangaza habari hizo katika mahekalu yao ya sanamu na
kwa watu. 10 Wakaziweka silaha zake katika hekalu la Ashtorethi, nao wakakitundika
kiwiliwili chake kwenye ukuta wa mji wa Bethi Shani. 11 Na wenyeji wa Yabeshi
Gileadi waliposikia kile Wafilisti walichomfanyia Sauli, 12 wapiganaji wote wakainuka
na kwenda usiku wote na wakauondoa mwili wa Sauli na miili ya wanawe kutoka
ukuta wa Bethi Shani. Nao wakaenda Yabeshi na wakaichoma moto hiyo miili huko.
13 Kisha wakachukua mifupa yao na kuizika chini ya mti wa mkwaju huko Yabeshi,
na wakafunga siku saba.

# 2 Samweli

1 Baada ya kifo cha Sauli, Daud alirudi kutoka kuwashambulia Waamaleki na
akakaa Siklagi kwa siku mbili. 2 Siku ya tatu, mtu mmoja alikuja kutoka kambi
ya Sauli nguo zake zikiwa zimeraruliwa na akiwa na vumbi juu ya kichwa chake.
Alipofika kwa Daudi alinamisha uso wake chini akajifanya yeye mwenyewe kuwa si
kitu. 3 Daudi akamuliza, “Unatoka wapi?” Yeye akajibu, “Nimeponyoka kutoka kambi
ya Israeli.” 4 Daudi akamwambia, “Tafadhari nieleze jinsi mambo yalivyokuwa.”
Akajibu, “Watu walikimbia kutoka vitani. Wengi wameanguka, na wengi wao
wameuawa. Sauli na Yonathani mwanawe pia wameuawa.” 5 Daudi akamwuliza
kijana, “unajuaje kuwa Sauli na Yonathani mwanawe wameuawa?” 6 Yule kijana
akajibu, “Kwa bahati nilikuwa juu ya Mlima Gilboa, na pale alikuwepo Sauli
ameegemea mkuki wake, na magari ya farasi na waongozaji walikuwa karibu
kumkamata. 7 Sauli alipogeuka aliniona na akaniita. Nikajibu, 'Mimi hapa.'
8 Akaniuliza, 'Wewe ni nani?' Nikamjibu, 'Mimi ni Mwamaleki,' 9 Akaniambia,
Tafadhari simama juu yangu uniuwe, kwa kuwa shida kubwa imenipata, lakini
uhai ungalimo ndani yangu.' 10 Hivyo nilisimama juu yake nikamuuwa, kwa maana
nilijua kwamba asingeweza kuishi baada ya kuwa ameanguka. Ndipo nikachukuwa
taji iliyokuwa juu ya kichwa chake na kikuku kilichokuwa mkononi mwake, na
nimevileta hapa kwako, bwana wangu.” 11 Kisha Daudi akararua mavazi yake, na
watu wote waliokuwa pamoja naye wakafanya vilevile. 12 Walilia, wakaomboleza
na kufunga mpaka jioni kwa ajili ya Sauli, Yonathani mwanawe, watu wa Yahwe,
na kwa ajili ya nyumba ya Israeli kwa maana wameanguka kwa upanga. 13 Daudi
akamwambia yule kijana, “Unatokea wapi?” Akajibu, mimi ni kijana wa mgeni
Mwamaleki.” 14 Daudi akamwambia, “Kwa nini haukuogopa kumwua mfalme, mtiwa
mafuta wa Yahwe kwa mkono wako?” 15 Daudi akamwita mmojawapo wa vijana
na akamwambia, “Nenda ukamuue.” Hivyo kijana huyo akaenda na kumpiga hata
ata chini, Mwamaleki akafa. 16 Ndipo Daudi akamwambia Mwamaleke aliyekufa,
“Damu yako iwe juu ya kichwa chako kwa kuwa kinywa chako kimeshuhudia dhidi
yako kusema, Nimemuua mfalme mtiwa mafuta wa Yahwe. 17 Ndipo Daudi akaimba
wimbo wa maombolezo juu ya Sauli na Yonathani mwanawe. 18 Akawaamuru
watu kuufundisha wimbo wa Bow kwa wana wa Yuda, ambao umeandikwa katika
Kitabu cha Yashari. 19 “Utukufu wako, Israel, umeondolewa, umeondolewa juu ya
mahali pako pa juu! Jinsi mwenye nguvu alivyoanguka! 20 Msiiseme katika Gathi,
msiitangaze katika mitaa ya Ashikeloni, ili binti za wafilisti wasifurahi, ili binti za
wasiotailiwa wasisherehekee. 21 Milima ya Gilboa, kusiwe na umande au mvua juu
yenu. wala mashamba yasitoe nafaka kwa ajili ya sadaka, kwa maana hapo ngao ya
mwenye nguvu imeharibiwa. Ngao ya Sauli haiwezi tena kutiwa mafuta. 22 Kutoka
katika damu ya waliouawa, kutoka katika miili ya wenye nguvu, upinde wa Yonathani
haukurudi nyuma, na upanga wa Sauli haukurudi patupu. 23 Sauli na Yonathani
walikuwa wakipendwa na walikuwa wenye neema maishani, hata wakati wa mauti
yao walikuwa pamoja. Walikuwa na kasi kuliko tai, walikuwa na nguvu kuliko simba.
24 Enyi binti wa Israeli lieni juu ya Sauli, aliyewavika mavazi ya thamani pamoja na
vito vya thamani, na aliyetia mapambo ya dhahabu katika mavazi yenu. 25 Jinsi
wenye nguvu walivyoanguka vitani! Yonathani ameuawa juu ya mahali pako pa juu.
26 Nimesikitishwa sana kwa ajili yako, Yonathani ndugu yangu. Ulikuwa mpendwa
wangu sana. Upendo wako kwangu ulikuwa wa ajabu, ukipita upendo wa wanawake.
27 Jinsi wenye nguvu walivyoanguka na silaha za vita zimeteketea!”

# 2

[1] Ikawa baada ya haya Daudi akamuuliza Yahwe, "Je naweza kuupandia mmo-
jawapo wa miji ya Yuda?" Yahweh akamjibu, "Panda." Daudi akauliza, "Niuendee
mji upi? Yahwe akajibu, "Hebroni" [2] Hivyo Daudi akakwea pamoja na wake zake
wawili, Ahinoamu wa Yezreeli, na Abigaili wa Karmeli, mjane wa Nabali. [3] Daudi
akawaleta watu waliokuwa pamoja naye, na kila mmoja akaleta familia yake katika
mji wa Hebroni walipoanza kuishi. [4] Kisha watu wa Yuda wakaja na kumtia Daudi
mafuta kuwa mfalme juu ya nyumba ya Yuda. Wakamwambia Daudi, "Watu wa
Yabeshi Gileadi wamemzika Sauli." [5] Hivyo Daudi akatuma wajumbe kwa watu wa
Yabeshi Gileadi akawambia, "Mbarikiwe na Yahwe, kwa kuwa mmeonesha utiifu huu
kwa bwana wenu Sauli mliyemzika. [6] Sasa Yahwe awadhihirishie utiifu na uaminifu
wa kiagano. Nami pia nitawaonesha wema kwa sababu ya yale mliyoyafanya. [7] Sasa
basi, mikono yenu itiwe nguvu; mwe jasiri kwa maana Sauli bwana wenu amekufa,
na nyumba yote ya Yuda imenitia mafuta niwe mfalime wao. [8] Lakini Abneri
mwana wa Neri, mkuu wa jeshi la Sauli, akamchukuwa Ishboshethi mwana wa
Sauli akamleta Mahanaimu. [9] Akamfanya Ishboshethi mfalme juu ya Gileadi, Asheri,
Yezreeli, Efraimu, Benjamini na juu ya Israeli yote. [10] Ishiboshethi mwana wa Sauli
alikuwa na umri wa miaka arobaini alipoanza kutawala juu ya Israeli, akatawala
miaka miwili. Lakini nyumba ya Yuda ikaambatana na Daudi. [11] Muda ambao Daudi
alikuwa mfalme juu ya nyumba ya Yuda huko Hebroni ni miaka saba na miezi sita.
[12] Abneri mwana wa Neri na watumishi wa Ishboshethi mwana wa Sauli walitoka
Mahanaimu kwenda Gibeoni. [13] Yoabu mwana wa Seruya na watumishi wa Daudi
wakatoka na kukutana nao katika bwawa la Gibeoni. Wakakaa pale, kundi moja
upande huu wa bwawa na kundi lingine upande wa pili. [14] Abneri akamwambia
Yoabu, "haya, vijana na wainuke na kushindana mbele yetu." Yoabu akajibu, "haya
na wainuke." [15] Ndipo vijana walipoinuka na kukutana, kumi na wawili kwa ajili ya
Banjamini na Ishboshethi mwana wa Sauli, na kumi na wawili kutoka kwa watumishi
wa Daudi. [16] Kila mtu akakamata kichwa cha adui yake na kupiga upanga wake katika
ubavu wa adui yake, wakaanguka chini pamoja. Kwa hiyo mahali pale pakaitwa kwa
Kiebrania, "Helkath Hazzurim," yaani "konde la upanga," lililopo Gibeoni. [17] Vita
ikawa kali sana siku ile na Abneri na watu wa Israeli wakashindwa na watumishi
wa Daudi. [18] Wana watatu wa Seruya walikuwepo pale: Yoabu, Abishai na Asaheli.
[19] Asaheli alikuwa mwepesi miguuni kama paa. Akamfuatilia Abneri kwa karibu
bila kugeuka upande wowote. [20] Abneri akaangalia nyuma yake na kusema, "Ni
wewe Asaheli?" Akajibu, "ni mimi." [21] Abneri akamwambia, "Geuka upande wako
wa kuria au kushoto umshike mmojawapo wa vijana na kuchukua silaha yake."
Lakini Asaheli hakugeuka. [22] Ndipo Abneri alipomwambia tena Asaheli, "Simama
usinifuate. Kwa nini nikupige hata chini? Nitautazamaje uso wa Yoabu ndugu
yako?" [23] Lakini Asaheli hakukubari kugeuka. na hivyo Abneri akamchoma kwa
nchi ya mkuki wake, hata ukatokea upande wa pili. Asaheli akaanguka chini akafa.
Hata ikawa kila mmoja aliyefika mahali pale Asaheli alipoanguka na kufa, alisimama
hapo hapo. [24] Lakini Yoabu na Abishai wakamfuatilia Abneri. Wakati jua linazama
walikuwa wamefika mlima wa Amma, uliopo karibu na Gia katika njia ielekeayo
nyika ya Gibeoni. [25] Wabenjamini wakajikusanya nyuma ya Abneri na kusimama
juu ya kilima. [26] Kisha Abneri akamwita Yoabu na kusema, "Je ni lazima upanga
uendelee kurarua daima? Je haujui kwamba mwisho wake utakuwa mchungu? Hata
line ndipo uwaambie watu wako waache kuwafuatia ndugu zao?" [27] Yoabu akajibu,
"Kama Mungu aishivyo, usingesema hivyo, askari wangu wangewafuatia ndugu zao
hata asubuhi!" [28] Ndipo Yoabu akapiga tarumbeta, na watu wake wote wakasimama
na hawakuendelea kuwafuata Israeli tena wala hawakupigana tena. [29] Abneri na

watu wake wakasafiri usiku wote kupitia Araba. Wakavuka Yordani, wakatembea
asubuhi yote iliyofuata, na hata wakafika Mahanaimu. 30 Yoabu akarudi kutoka
katika kumfuatia Abneri. Akawakusanya watu wake wote, ambopo Asahali na askari
wengine kumi na tisa wa Daudi walipungua. 31 Lakini watu wa Daudi walikuwa
wameua watu 360 wa Benjamini na Abneri. 32 Kisha wakamchukua Asahali na
kumzika katika kaburi la baba yake, lililokuwapo Bethlehemu. Yoabu na watu wake
wakasafiri usiku wote, kukacha wakati wanafika Hebroni.

# 3

1 Kulikuwa na vita ya mda mrefu kati ya nyumba ya Sauli na nyumba ya Daudi.
Daudi akaendelea kupata nguvu zaidi, lakini nyumba ya Sauli iliendelea kudhoofika
na kuthoofika. 2 Wana wakazaliwa kwa Daudi huko Hebron. Mzaliwa wake wa
kwanza alikuwa Amnoni, kwa Ahinoamu wa Yezreeli. 3 Mwanawe wa pili, Kileabu,
alizaliwa kwa Abigaili, mjane wa Nabali wa Karmeli. Wa tatu, Absalomu, alikuwa
mwana wa Maaka, binti Talmai, mfalme wa Geshuri. 4 Mwana wa nne wa Daudi,
Adoniya, alikuwa mwana wa Hagithi. Mwanawe wa tano alikuwa Shefatia mwana
wa Abitali, 5 na wa sita, Ithreamu, alikuwa mwana wa Egla mkewe Daudi. Hawa
wote walizaliwa kwa Daudi huko Hebroni. 6 Ikawa wakati wa vita kati ya nyumba
ya Sauli na nyumba ya Daudi Abneri akajifanya mwenye nguvu katika nyumba ya
Sauli. 7 Sauli alikuwa na suria jina lake Rispa, binti Aiya. Ishboshethi akamuuliza
Abneri, “Kwa nini umelala na suria wa baba yangu?” 8 Hata ikawa Abneri akakasirika
sana kutokana na maneno ya Ishboshethi naye akasema, “Je mimi ni kichwa cha
mbwa wa Yuda? Ninaonesha uaminifu kwa nyumba ya Sauli, baba yako, kwa jamaa
yake, na rafiki zake, kwa kutokukuweka katika mkono wa Daudi. Na bado leo
unanishutumu kuhusu mwanamke. 9 Mungu na anifanyie hivyo, Abneri, na kuzidi,
ikiwa sitafanya kwa Daudi kama Yahwe alivyomwapia, 10 kuuhamisha ufalme kutoka
nyumba ya Sauli na kukisimika kiti cha enzi cha Daudi juu ya Israeli na juu ya
Yuda, kutoka Dani hadi Beersheba.” 11 Ishboshethi hakuweza kumjibu Abneri neno
tena, kwani alimuogopa. 12 Kisha Abneri akatuma wajumbe kwa Daudi kusema,
“Nchi hii ni ya nani? Fanya agano nami, nawe utaona kwamba mkono wangu
uko nawe, kuiIeta Israeli yote kwako.” 13 Daudi akajibu, “Vema, nitafanya agano
nawe. Lakini neno moja ninalolitaka kutoka kwako ni kwamba hautauona uso wangu
usipomuleta kwanza Mikali, binti Sauli, unapokuja kuonana nami.” 14 Kisha Daudi
akatuma wajumbe kwa Ishboshethi, mwana wa Sauli, kusema, “Nipe Mikali, mke
wangu niliyetoa kwa ajili yake govi mia moja za Wafilisti.” 15 Hivyo Ishboshethi
akatuma kwa Mikali na kumchukua kutoka kwa mme wake, Paltieli mwana wa
Laishi. 16 Mme wake akafuatana naye, huku akilia, akaendelea hadi Bahurimu.
Kisha Abneri akamwambia, “basi sasa rudi nyumbani.” Hivyo akarudi. 17 Abneri
akaongea na wazee wa Israeli kusema, “Zamani mlitaka Daudi awe mfalme wenu.
18 Basi sasa fanyeni hivyo. Kwa maana Yahwe alisema kuhusu Daudi kusema, “Kwa
mkono wa Daudi mtumishi wangu nitawaokoa watu wangu Israeli kutoka katika
mkono wa Wafilisti na kutoka katika mkono wa adui zao wote.” 19 Pia Abneri
akasema na watu wa Benjamini ana kwa ana. Kisha Abneri akaenda kuongea
na Daudi huko Hebroni akaeleza kila jambo ambalo Israeli na nyumba yote ya
Benjamini walitamani kulitimiza. 20 Wakati Abneri na watu ishirini kati ya watu
wake walifika Hebroni kumuona Daudi, Daudi akaandaa sherehe kwa ajili yao.
21 Abneri akamweleza Daudi, “Nitainuka na kukukusanyia Israeli wote, bwana wangu
mfalme, ili kwamba wafanye agano nawe, kwamba utawale juu ya yote unayotaka.”
Hivyo Daudi akamruhusu Abneri kuondoka, Abneri akaondoka kwa amani. 22 Kisha
askari wa Daudi na Yoabu wakarudi kutoka katika kuteka nyara na wakaja na

nyara nyingi. Lakini Abneri hakuwepo Hebroni pamoja na Daudi. Daudi alikuwa
amemruhusu kuondoka, na alikuwa ameondoka kwa amani. 23 Wakati Yoabu na
Jeshi lote walipofika, Yoabu aliambiwa, “Abneri mwana wa Neri alikuja kwa mfalme,
na mfalme amemruhusu kuondoka, naye Abneri ameondoka kwa amani.” 24 Kisha
Yoabu akaja kwa mfalme na kusema, “Umefanya nini? Tazama, Abneri alikuja
kwako! Kwa nini umemruhusu kuondoka, naye amenda? 25 Haujui kwamba Abneri
mwana wa Neri alikuja kukudanganya na kupeleleza hali yako na kuangalia kila
unalofanya?” 26 Yoabu alipoondoka kwa Daudi, alituma wajumbe kumfuatia Abneri,
nao wakamrudisha kutoka katika kisima cha Sirah, lakini Daudi hakulijua hili.
27 Abneri aliporudi Hebroni, Yoabu alimchukua kando kati ya lango ili aongee naye
faraghani. Hapohapo Yoabu alimchoka tumboni na kumuua. Hivyo, akalipa kisasi
cha damu ya Asaheli nduguye. 28 Daudi alipolisikia jambo hili akasema, “Mimi na
ufalme wangu hatuna hatia mbele za Yahwe daima, kuhusiana na damu ya Abneri
mwana wa Neri. 29 Hatia ya damu ya Abneri na iwe juu ya Yoabu na nyumba yote ya
baba yake. Na asikosekane katika familia ya Yoabu mtu mwenye vidonda, au mwenye
ukoma, au kirema atembeaye kwa fimbo au aliyeuawa kwa upanga au mwenye
kukosa chakula.” 30 Hivyo Yoabu na Abishai nduguye wakamwua Abneri, kwa sababu
alimwua Asaheli ndugu yao vitani huko Gibeoni. 31 Daudi akamwambia Yoabu na
wote waliokuwa pamoja naye, “Rarueni mavazi yenu, jivikeni nguo za magunia, na
muomboleze mbele ya mwili wa Abneri.” Na mfalme Daudi akaufuata mwili wa
Abneri wakati wa mazishi. 32 Wakamzika Abneri huko Hebroni. Mfalme akalia kwa
sauti katika kaburi la Abneri, na watu wote pia wakalia. 33 Mfalme akamwombolea
Abneri naye akaimbo, “Je ilipasa Abneri afe kama afavyo mpumbavu? 34 Mikono yako
haikufungwa. Miguu yako hakuwa imefungwa minyororo. Kama mtu aangukavyo
mbele ya wana wa uovu, ndivyo ulivyoanguka.” Watu wote wakamlilia zaidi.
35 Watu wote wakaja kumtaka Daudi ale wakati kungali mchana, lakini Daudi akaapa,
“Mungu na anifanyie hivyo, na kuzidi, ikiwa nitaonja mkate au chochote kabla jua
halijazama.” 36 Watu wote wakaiona huzuni ya Daudi, na ikawapendeza, hivyo
kila alichokifanya mfalme kikawapendeza. 37 Hivyo watu wote na Israeli wote
wakatambua siku hiyo kwamba haikuwa nia ya mfalme Abneri mwana wa Neri afe.
38 Mfalme akawaambia watumishi wake, “je hamjui kuwa mtu mkuu ameanguka
leo hii katika Israeli? 39 Nami leo nimedhoofika, japokuwa nimetiwa mafuta kuwa
mfalme. Watu hawa, wana wa Seruya ni hatari sana kwangu. Yahwe na amrudishie
mwovu kwa kumlipa kwa ajili ya uovu wake kama anavyostahili.

# 4

1 Ikawa Ishboshethi, mwana wa Sauli, aliposikia kwamba Abneri amekufa huko
Hebroni, mikono yake ikadhoofika, na Israeli yote ikataabika. 2 Basi mwana wa
Sauli alikuwa na watu wawili waliokuwa wakuu wa vikosi vya askari. Mmoja
wao alikuwa Baana na mwingine alikuwa Rekabu, wana wa Rimoni Mbeerothi wa
wana wa Benjamini(kwa maana Berothi ilihesabiwa kuwa sehemu ya Benjamini,
3 na Waberothi walikimbilia Gitaimu na wamekuwa wakiishi pale hadi sasa). 4 Basi
Yonathani, mwana wa Sauli, alikuwa na mwana mlemavu wa miguu. Alikuwa na
umri wa miaka mitano habari kuhusu Sauli na Yonathani ilipofika Yezreeli. Yaya
wake akamchukua ili akimbie. Lakini wakati anakimbia, mwana wa Yonathani
alianguka na akawa kirema. Jina lake aliitwa Mefiboshethi. 5 Hivyo wana wa
Rimoni mbeerothi, Rekabu na Baana, wakasafiri mchana wakati wa jua kali mpaka
nyumbani mwa Ishbothethi, yeye alikuwa amepumzika mchana. 6 Mwanamke
aliyekuwa akililinda lango alisinzia wakati akipepeta ngano, Rekabu na Baana
waliingia ndani polepole na wakampita. 7 Hivyo walipoingia ndani ya nyumba,

walimpiga na kumuua wakati amelala chumbani mwake. Kisha wakakata kichwa
chake na wakaondoka nacho, wakasafiri njiani usiku kucha mpaka Araba. 8 Wakaleta
kichwa cha Ishboshethi kwa Daudi huko Hebroni, nao wakamwambia mfalme,
"Tazama, hiki ni kichwa cha Ishboshethi mwana wa Sauli, adui yako, aliyekuwa
akiutafuta uhai wako. Leo Yahwe amemlipia kisasi bwana wetu mfalme dhidi ya
Sauli na uzao wake." 9 Daudi akawajibu Rekabu na Baana nduguye, wana wa Rimoni
mbeerothi, akawambia, "Kama Yahwe aishivyo, aliyeuokoa uhai wangu na kila shida,
10 mtu mmoja aliponiambia, 'Tazama, Sauli amekufa,' akifikiri alileta habari njema,
nilimkamata na kumwua huko Siklagi. Huo ndio ujira niliompa kwa habari yake.
11 Namna gani, mtu mwovu anapomwua mwenye haki kitandi mwake ndani ya
nyumba, Je nisiitake damu yake kutoka katika mikono yenu, na kuwaondoa duniani?"
12 Kisha Daudi akawaagiza vijana, nao wakawaua wakakata mikono na miguu yao
na kuwatundika kando ya bwawa huko Hebroni. Lakini wakakichukua kichwa cha
Ishboshethi na kukizika katika kaburi la Abneri katika Hebroni.

# 5

1 Kisha kabila zote za Israeli wakamwendea mfalme huko Hebroni nao wakasema,
"Tazama, sisi ni nyama na mifupa yako. 2 Kipindi kilichopita, Sauli alipokuwa
mfalme juu yetu, ni wewe uliyeliongoza jeshi la Waisraeli. Yahwe akakwambia,
'Utawachunga watu wangu Israeli, na utakuwa mtawala juu ya Israeli." 3 Hivyo
wazee wote wa Israeli wakaja kwa mfalme huko Hebron na mfalme Daudi akafanya
nao agano mbele ya Yahweh. Wakamtawaza Daudi kuwa mfalme wa Israeli. 4 Daudi
alikuwa na umri wa miaka thelathini alipoanza kutawala, naye akatawala miaka
arobaini. 5 Alitawala juu ya Yuda miaka saba na miezi sit a huko Hebroni, na
huko Yerusalemu akatawala miaka thelathini na mitatu juu ya Israeli yote na Yuda.
6 Mfalme na watu wake wakaenda Yerusalemu kupigana na wayebusi, waliokuwa
wenyeji wa nchi. Wakamwambia Daudi, "Hautaweza kuja hapa kwani hata wipofu
na vilema waweza kukudhuia kuingia. Daudi haweze kuja hapa." 7 Lakini, Daudi
akaiteka ngome ya Sayuni, ambayo sasa ni mji wa Daudi. 8 Wakati huo Daudi
akasema, "Waliowashambulia wayebusi watapaswa kupita katika mfereji wa maji
ili wawafikie virema na vipofu ambao ni adui wa Daudi." Hii ndiyo maana watu
husema, "Vipofu na virema wasingie katika kasri." 9 Hivyo Daudi akaishi ngemeni
naye akaiita mji wa Daudi. Akaizungushia ukuta, kuanzia barazani kuelekea ndani.
10 Daudi akawa na nguvu sana kwa maana Yahwe, Mungu wa utukufu, alikuwa
pamoja naye. 11 Kisha Hiramu mfalme wa Tiro akatuma wajumbe kwa Daudi, na miti
ya mierezi, mafundi seremala na wajenzi. Wakamjengea Daudi nyumba. 12 Daudi
akatambua kuwa Yahwe alikuwa amemweka ili awe mfalme juu ya Israeli, na
kwamba alikuwa ameutukuza ufalme wake kwa ajili ya Israeli watu wake. 13 Baada
ya Daudi kuondoka Hebroni na kwenda Yerusalemu, akajitwalia wake na masuria
wengi huko Yerusalemu, na wana na binti wengi walizaliwa kwake. 14 Haya ndiyo
majina ya wanawe waliozaliwa kwake huko Yerusalemu: Shamua, Shobabu, Nathani,
Selemani, 15 Ibhari, Elishua, Nefegi, Yafia, 16 Elishama, Eliada na Elifeleti. 17 Basi
wafilisti waliposikia kwamba Daudi ametiwa mafuta kuwa mfalme juu ya Israeli,
wakaenda wote kumtafuta. Daudi aliposikia hilo akashuka ngomeni. 18 Basi Wafilisiti
walikuwa wamekuja na kuenea katika bonde la Mrefai. 19 Kisha Daudi akaomba
msaada kutoka kwa Yahwe. Akasema, "Je niwashambulie wafilisti? Je utanipa
ushindi juu yao?" Yahwe akamwambia Daudi, "Washambulia, kwa hakika nitakupa
ushindi juu ya wafilisti." 20 Hivyo Daudi akawashambulia huko Baali Perasimu,
naye akawashinda. Akasema, Yahwe amewafurikia adui zangu mbele yangu kama
mafuriko ya maji. Kwa hiyo jina la mahali pale likawa Baali Perasimu. 21 Wafilisiti

wakaacha vinyago vyao pale, na Daudi na watu wake wakaviondoa. 22 Kisha wafilisiti
wakaja kwa mara nyingine tena na kujieneza zaidi katika bonde la Mrefai. 23 Hivyo
Daudi akatafuta msaada tena kutoka kwa Yahweh, naye Yahweh akamwambia,
“Usiwashambulie kwa mbele, lakini uwazunguke kwa nyuma na uwaendee kupitia
miti ya miforosadi. 24 Wakati utakaposikia sauti za mwendo katika upepo uvumao
juu ya miti ya miforosadi, hapo ushambulie kwa nguvu. Fanya hivi kwa kuwa
Yahwe atatangulia mbele yako kulishambulia jeshi la Wafilisiti.” 25 Hivyo Daudi
akafanya kama Yahwe alivyomwamuru. Akawaua wafilisti njiani mwote toka Geba
hadi Gezeri.

# 6

1 Basi kwa mara nyingine Daudi akawakusanya wateuli wa Israeli, elfu thelathini.
2 Daudi akainuka na akaenda na watu wake wote waliokuwa pamoja naye kutoka
Baala ulioko Yuda ili alilete sanduku la Mungu, liitwalo kwa jina la Yahwe wa majeshi,
akaaye juu ya makerubi. 3 Wakaliweka sanduku la Mungu juu ya mkokoteni mpya.
Wakalitoa katika nyumba ya Abinadabu, iliyokuwa juu ya kilima. Uza na Ahio,
wanawe, wakauongoza mkokoteni. 4 Wakautoa mkokoteni na sanduku la Mungu
juu yake nyumbani mwa Abinadabu juu ya kilima. Ahio alikuwa ametangulia mbele
ya sanduku. 5 Kisha Daudi na nyumba yote ya Israeli wakaanza kucheza mbele ya
Yahwe, wakishangilia kwa vyombo vya mziki, vinubi, vinanda, matari, kayamba na
matowazi. 6 Hata walipofika katika shinikizo la Nasoni, wale ng'ombe wakakwama,
Uza akanyosha mkono wake na kulikumbatia sanduku la Mungu, naye akalishikilia.
7 Kisha asira ya Yahweh ikawaka dhidi ya Uza. Mungu akampiga kwa ajili ya dhambi
yake. Uza akafa pale pale kando ya sandaku la Mungu. 8 Daudi akakasirika kwa
kuwa Yahwe alimpiga Uza, naye akapaita mahali pale Peresi Uza. Eneo hilo linaitwa
Peres Uza hata leo. 9 Daudi akamwogopa Yahweh siku hiyo. Akasema, “Sanduku
la Yahwe lawezaje kuja kwangu?” 10 Hivyo Daudi hakuwatayari tena kulichukua
sanduku la Yahwe katika mji wa Daudi. Badala yake, akaliweka kando katika nyumba
ya Obedi Edomu Mgiti. 11 Sanduku la Yahwe likakaa katika nyumba ya Obedi Edomu
Mgiti kwa miezi mitatu. Kwa hiyo Yahwe akambariki yeye na nyumba yake yote.
12 Kisha mfalme Daudi akaambiwa, “Yahwe ameibariki nyumba ya Obedi Edomu
na kila kitu alichonacho kwa sababu ya sanduku la Mungu.” Hivyo Daudi akaenda
na kulipandisha sanduku la Mungu kutoka katika nyumba ya Obedi Edomu hadi
mji wa Daudi kwa furaha. 13 Ikawa waliolibeba sanduku la Yahwe walipochukua
hatua sita, akatoa sadaka ng'ombe na ndama aliyenona. 14 Daudi akacheza mbele ya
Yahwe kwa nguvu zake zote; alikuwa amevaa naivera ya kitani pekee. 15 Hivyo Daudi
na nyumba yote ya Israeli wakalipandisha sanduku la Yahwe kwa vifijo na sauti
za tarumbeta. 16 Hata ikawa sanduku la Yahwe lilipofika mjini mwa Daudi, Mikali,
binti Sauli, alichungulia dirishani. Akamwona mfalme Daudi akiruka na kucheza
mbele ya Yahwe. Akamdharau moyoni mwake. 17 Wakaliingiza sanduku la Yahwe na
kuliweka mahali pake, katikati ya hema ambayo Daudi alikuwa ameliwekea. Kisha
Daudi akatoa sadaka ya kuteketezwa na matoleo ya amani mbele za Yahwe. 18 Ikawa
Daudi alipomaliza kutoa sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani, akawabariki
watu kwa jina la Yahwe wa majeshi. 19 Kisha akawagawia watu wote, umati wote
wa Israeli, wanaume kwa wanawake, kipande cha mkate, nyama na keki ya zabibu.
Kisha watu wote wakaondoka; kila mmoja akarudi kwake. 20 Kisha Daudi akarudi ili
aibariki familia yake. Mikali, binti Sauli, akatoka ili akutane na Daudi naye akasema,
“Jinsi gani mtukufu mfalme wa Israeli alivyokuwa leo, aliyejiacha uchi mbele ya
macho ya vijakazi miongoni mwa watumishi wake, kama mmoja wa wapumbavu
ambaye bila aibu hujifunua yeye mwenyewe!” 21 Daudi akamjibu Mikali, “Nilifanya

hivyo mbele ya Yahwe, aliyenichagua juu ya baba yako na juu ya familia yake yote,
aliyeniweka kuwa kiongozi juu ya watu wa Yahwe, juu ya Israeli. Mbele ya Yahwe
nitafurahi! 22 Nitakuwa nisiye na heshima hata zaidi ya hapa, na nitajishusha mbele
za macho yangu mwenyewe. Lakini kwa hawa vijakazi uliowasema, nitaheshimiwa."
23 Hivyo Mikali, binti Sauli, hakuwa na watato hata alipokufa.

# 7

1 Ikawa mfalme alipokuwa amekwisha kukaa katika nyumba yake, na baada ya
Yahwe kuwa amemstarehesha kutokana na adui zake wate waliomzunguka, 2 mfalme
akamwambia nabii Nathani, "Tazama, mimi ninaishi katika nyumba ya mierezi,
lakini sanduku la Mungu lipo hemani. 3 Basi Nathani akamwambia mfalme, "Nenda,
fanya lililo moyoni mwako, kwa maana Yahwe yupo nawe." 4 Lakini usiku usiku
uleule neno la Yahwe lilimjia Nathani kusema, 5 "Nenda na umwambie mtumishi
wangu Daudi, 'Hivi ndivyo asemavyo Yahwe: Je utanijengea nyumba ya kuishi?"
6 Kwa maana sijawai kuishi katika nyumba tangu siku ile nilipowaleta wana wa
Israeli kutoka Misri hata leo; badala yake nimekuwa nikitembea katika hema, hema
la kukutania. 7 Mahali pote ambapo nimekuwa nikihama miongoni mwa wana wote
wa Israeli, Je niliwai kusema lolote na viongozi wa Israeli niliowaweka kuwachunga
watu wangu Israeli, kusema, "Kwa nini hamjanijengea nyumba ya mierezi?" 8 Sasa
basi, mwambie Daudi, mtumishi wangu, "Hiki ndicho asemacho Yahwe wa majeshi:
'Nilikutwaa kutoka machungani, kutoka katika kuwafuata kondoo, ili uwe mtawala
juu ya watu wangu Israeli. 9 Nimekuwa pamoja nawe popote ulipokwenda na
nimewakatilia mbali adui zako wote mbele yako. Na nitakutengenezea jina kubwa,
kama jina la mojawapo ya wakuu walio juu ya nchi. 10 Nitatenga mahali kwa
ajili ya watu wangu Israeli nami nitawapanda pale, ili kwamba waweze kuishi
mahali pao wenyewe na wasisumbuliwe tena. Waovu hawatawatesa tena, kama
walivyofanya mwanzo. 11 Kama walivyofanya tangu siku ile nilipoamuru waamuzi
juu ya watu wangu Israeli. Nami nitakustarehesha kutokana na adui zako wote.
Zaidi ya hayo, Mimi, Yahwe, nakutamkia kwamba nitakutengenezea nyumba. 12 Siku
zako zitakapokwisha na ukalala pamoja na baba zako, nitainua mzao baada yako,
atokaye katika mwili wako mwenyewe, nitauimalisha ufalme wake. 13 Naye atajenga
nyumba kwa jina langu, nami nitakiimalisha kiti chake cha enzi daima. 14 Nitakuwa
baba kwake, naye atakuwa mwanangu. Atakapotenda dhambi, nitamwadhibu kwa
fimbo ya wanadamu na kwa mapigo ya wana wa watu. 15 Lakini uaminifu wa agano
langu hautamwondokea, kama nilivyouondoa kutoka kwa Sauli, niliyemwondoa
mbele yako. 16 Nyumba yako na ufalme wako utathibitiswa mbele yako daima.
Kiti chako cha enzi kitakuwa imara daima." 17 Nathani akamwambia Daudi na
kumtaarifu maneno haya yote, na akamwambia kuhusu ono lote. 18 Kisha mfalme
Daudi akaingia ndani na kuketi mbele ya Yahwe; akasema, "Mimi ni nani, Yahwe
Mungu, na familia yangu ni nini hata umenileta hapa nilipo? 19 Na hili lilikuwa jambo
dogo mbele yako, Bwana Yahwe. Hata ukasema kuhusu familia ya mtumishi wako
wakati mkuu ujao, nawe umenionesha vizazi vijavyo, Bwana Yahwe! 20 Mimi Daudi,
niseme nini zaidi kwako? Umemweshimu mtumishi wako, Bwana Yahwe. 21 Kwa
ajili ya neno lako, na kwa ajili ya kutimiza kusudi lako mwenyewe, umefanya jambo
kubwa namna hii na kulidhihirisha kwa mtumishi wako. 22 Kwa hiyo wewe ni mkuu,
Bwana Yahwe. Kwa maana hakuna mwingine aliye kama wewe, na hakuna Mungu
mwingine badala yako, kama jinsi ambayo tumesikia kwa masikio yetu wenyewe.
23 Kwani kuna taifa lipi lililo kama watu wako Israeli, taifa moja juu ya nchi ambalo
wewe, Mungu, ulikwenda na kuwakomboa kwa ajili yako wewe mwenyewe? Ulifanya
hivi ili kwamba wawe watu kwa ajili yako mwenyewe, kujifanyia jina kwa ajili yako

mwenyewe, na kufanya matendo makuu na ya kuogofya kwa ajili ya nchi yako.
Uliyaondoa mataifa na miungu yao kutoka mbele ya watu wako, uliowakomboa
kutoka Misri. [24] Umeiimarisha Israel kama watu wako daima, na wewe, Yahwe, kuwa
Mungu wao. [25] Basi sasa, Yahwe Mungu, ahadi uliyofanya kuhusu mtumishi wako na
familia yake iwe imara daima. Ufanye kame uilivyo sema. [26] Na jina lako liwe kuu
daima, ili watu waseme, 'Yahwe wa majeshi ni Mungu wa Israeli,' wakati nyumba
yangu, Daudi, mtumishi wako itakapokaa imara mbele zako daima. [27] Kwa maana
wewe, Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli, umedhihirisha kwa mtumishi wako
kwamba utamjengea nyumba. Ndiyo maana mimi, mtumishi wako, nimepata ujasiri
kuomba kwako. [28] Sasa, Bwana Yahwe, wewe ni Mungu, na maneno yako ni amini, na
umefanya ahadi hii njema kwa mtumishi wako. [29] Sasa basi, na ikupendeze kuibariki
nyumba ya mtumishi wako, ili iendelee mbele yako daima. Kwa maana wewe, Bwana
Yahwe, umeyasema mambo haya, na kwa ahadi yako nyumba ya mtumishi wako
itabarikiwa daima.

# 8

[1] ikawa baada ya haya Daudi aliwashambulia Wafilisti na kuwashinda. Hivyo
Daudi akaichukua Gathi na vijiji vyake kutoka katika mamlaka ya wafilisti. [2] Kisha
akaishinda Moabu na akawapima watu wake kwa mstari kwa kuwafanya walale
chini juu ya ardhi. Alipima mistari miwili ya kuua, na mstari mmoja kamili
kuwahifadhi hai. Hivyo Wamoabu wakawa watumishi wa Daudi na wakaanza
kumlipa kodi. [3] Kisha Daudi akamshinda Hadadezeri mwana wa Rehobu, mfalme
wa Soba, Hadadezeri aliposafiri kuurudisha ufalme wake katika mto Frati. [4] Daudi
aliteka magari 1, 700 ya farasi na askari ishirini elfu waendao kwa miguu. Daudi
akawakata miguu farasi wa magari, lakini akahifadhi wakutosha magari mia moja.
[5] Wakati Washami wa Dameski walipokuja kumsaidia Hadadeziri mfalme wa Soba,
Daudi akaua katika Washami watu ishirini na mbili elfu. [6] Daudi akaweka ngome
huko Shamu ya Dameski, na Washami wakawa watumishi wake na wakaleta kodi.
Yahwe akampa Daudi ushindi kila alikokwenda. [7] Daudi akachukua ngao za
dhahabu walizokuwa nazo watumishi wa Hadadezeri naye akazileta Yerusalemu.
[8] Mfalme Daudi akachukua shaba nyingi kutoka Beta na Berosai, miji ya Hadadezeri.
[9] Wakati Tou, mfalme wa Hamathi, aliposikia kwamba Daudi amelishinda jeshi lote
la Hadadezeri, [10] Tou akamtuma Hadoramu mwanawe kwa mfalme Daudi kumpa
salamu na kumbariki, kwa kuwa Daudi alikuwa amepigana na Hadadezeri na
kumshinda, maana Hadadezeri alikuwa amepiga vita dhidi ya Tou. Hadoramu akaja
pamoja na vitu vya fedha, dhahabu, na shaba. [11] Mfalme Daudi akaviweka wakfu vitu
hivi kwa ajili ya Yahwe, pamoja na fedha na dhahabu kutoka katika mataifa yote
aliyokuwa ameyashinda- [12] kutoka Shamu, Moabu, Waamoni, Wafilist, Waamaleki,
pamoja na nyara zote alizoziteka kutoka kwa Hadadezeri mwana wa Rehobu, mfalme
wa Soba. [13] Jina la Daudi likajulikana sana alipowashinda washami katika bonde la
Chumvi, pamoja na watu wao wapatao elfu kumi na nane. [14] Akaweka ngome katika
Edomu yote, na Waedomu wote wakawa watumishi wake. Yahwe akampa Daudi
ushindi kila alipokwenda. [15] Daudi akatawala juu ya Israeli yote, naye akatenda
kwa haki na usawa kwa watu wote. [16] Yoabu mwana wa Seruya alikuwa mkuu wa
jeshi, na Yehoshafati mwana wa Ahiludi alikuwa mwenye kuandika taarifa. [17] Sadoki
mwana wa Ahitubu na Ahimeleki mwana wa Abiathari walikuwa makuhani, na
Seraya alikuwa mwandishi. [18] Benaya mwana wa Yehoyada alikuwa juu ya Wakerethi
na Wapelethi, na wana wa Daudi walikuwa washauri wa mfalme.

# 9

[1] Daudi akasema, “Je kuna yeyote aliyesalia wa familia ya Sauli ambaye naweza
kumwonyesha kwa fadhiri kwa ajili ya Yonathani? [2] Alikuwepo mtumishi katika
familia ya Sauli jina lake Siba, akaitwa kwa Daudi. Mfalme akamuuliza, “Je wewe
ndiye Siba?” Akajibu, “Mimi ni mtumishi wako, ndiye.” [3] Hivyo mfalme akasema,
“Je hakuna aliyesalia wa familia ya Sauli ambaye naweza kumuonesha wema wa
Mungu?” Siba akamjibu mfalme, “Yonathani ana mwana, ambaye ni mlemavu wa
miguu. [4] Mfalme akamwambia, “Yupo wapi?” Siba akamjibu mfalme, “Tazama,
yupo katika nyumba ya Makiri mwana wa Amieli huko Lo Debari. [5] Ndipo mfalme
Daudi akatuma watu na kumtoa katika nyumba ya Makiri mwana wa Amieli huko
Lo Debari. [6] Hivyo Mefiboshethi mwana wa Yonathani mwana wa Sauli, akaja kwa
Daudi naye akainama uso wake hadi katika sakafu kwa kumheshimu Daudi. Daudi
akasema, “Mefiboshethi.” Naye akajibu, “Angalia, mimi ni mtumishi wako! [7] Daudi
akamwambia, “Usiogope, maana hakika nitakufadhiri kwa ajili ya Yonathani baba
yako, nami nitakurudishia ardhi yote ya Sauli babu yako, nawe utakula katika meza
yangu daima.” [8] Mefiboshethi akainama na kusema, “Mtumishi wako ni nani, hata
ukamwangalia kwa fadhiri mbwa mfu kama nilivyo?” [9] Kisha mfalme akamwita
Siba, mtumishi wa Sauli, na kumwambia, “Yote yaliyo ya Sauli na familia yake
nimempa mjukuu wa bwana wako. [10] Wewe, wanao, na watumishi wako mtalima
mashamba kwa ajili yake nanyi mtavuna mazao ili kwamba mjukuu wa bwana wako
apate chakula. Kwa maana Mefiboshethi, mjukuu wa bwana wako, atakula katika
meza yangu daima.” Basi Siba alikuwa na wana kumi na watano na watumishi
ishirini. [11] Kisha Siba akamwambia mfalme, “Mtumishi wako atafanya yote ambayo
bwana wangu mfalme amemwamuru mtumishi wake.” Mfalme akaongeza kusema,
kwa Mefiboshethi yeye atakula katika meza yangu, kama mmojawapo ya wana
wa mfalme.” [12] Mefiboshethi alikuwa na mwana mdogo jina lake Mika. Na wote
waliokuwa wanaishi katika nyumba ya Siba walikuwa watumishi wa Mefiboshethi.
[13] Hivyo Mefiboshethi akaishi Yerusalemu, naye akala chakula cha daima katika meza
ya mfalme, japokuwa alikuwa mlemavu wa miguu yote.

# 10

[1] Ikawa baadaye mfalme wa watu wa Amoni akafa, na Hanuni mwanaye akawa
mfalme mahali pake. [2] Daudi akasema, “Nitaonesha fadhiri Hanuni mwana wa
Nahashi, kwa kuwa baba yake alinifadhiri.” Hivyo Daudi akatuma watumishi wake
kumfariji Hanuni kwa habari ya baba yake. Watumishi wake wakaingia katika nchi
ya watu wa Amoni. [3] Lakini viongozi wa watu wa Amoni wakamwambia Hanuni
bwana wao, “Je unathani kwa hakika Daudi anamweshimu baba yako hata ametuma
watu kukutia moyo? Daudi hajawatuma watumishi wake kwako ili kuuangalia mji,
kuupeleleza, ili kuupindua? [4] Hivyo Hanuni akawachukuwa watumishi wa Daudi,
akawanyoa nusu ya ndevu zao, akachana mavazi yao hadi kwenye matako, naye
akawaacha waende zao. [5] Daudi alipoelezwa kuhusu hili, akatuma watu kwenda
kuwalaki, kwa kuwa walikuwa wamefedheheshwa sana. Mfalme akawambia, “Kaeni
Yeriko mpaka ndevu zenu zitakapoota, ndipo mrudi.” [6] Watu wa Amoni walipoona
kwamba wamenuka kwa Daudi, wakatuma wajumbe na kuwaajiri Washami wa Bethi
Rehobu na Soba, askari elfu ishirini waendao kwa mguu, na mfalme wa Maaka
pamoja na watu elfu, na watu wa Tobu elfu kumi na mbili. [7] Daudi aliposikia,
akamtuma Yoabu na jeshi lote la askari. [8] Waamoni wakatoka na wakafanya mistari
ya vita katika maingilio ya lango la mji wao, wakati Washami wa Soba na wale wa
Rehobu, na watu wa Tobu na Maaka, wakasimama peke yao uwandani. [9] Yoabu
alipoona mistari ya vita ikimkabili pote mbele na nyuma, alichagua baadhi ya

waisraeli wajuao kupigana vizuri na akawapanga dhidi ya Washami. 10 Na sehemu
iliyosalia ya jeshi, akawaweka chini ya Abishai nduguye, naye akawaweka katika
mistari ya vita dhidi ya jeshi la Amoni. 11 Yoabu akasema, “ikiwa Washami watakuwa
na nguvu zaidi juu yangu, kisha wewe, Abishai, lazima uniokoe. Lakini ikiwa jeshi
la Amoni litakuwa na nguvu zaidi juu yako, nitakuja kukuokoa. 12 Iweni na nguvu,
nasi tujioneshe kuwa wenye nguvu kwa ajili ya watu wetu na miji ya Mungu wetu,
kwa maana Yahwe atatenda yapendezayo kwa ajili ya kusudi lake. 13 Hivyo Yoabu na
askari wa jeshi lake wakasonga mbele katika vita dhidi ya Washami, waliolazimika
kukimbia mbele ya jeshi la Israeli. 14 Jeshi la Amoni lilipoona kwamba Washami
wamekimbia, nao pia wakakimbia kutoka kwa Abishai wakarudi ndani ya mji. Ndipo
Yoabu akarudi kutoka kwa watu wa Amoni na akarejea Yerusalemu. 15 Washami
walipoona kwamba wameshindwa na Israeli, walijikusanya pamoja tena. 16 Kisha
Hadareza akatuma kuleta vikosi vya Washami ng'ambo ya Mto Frati. Wakaja Helamu
pamoja na Shobaki, mkuu wa jeshi la Hadareza juu yao. 17 Daudi alipoambiwa,
aliwakusanya Israeli wote pamoja, akavuka Yordani, na akafika Helamu. Washami
wakajipanga katika mistari ya vita dhidi ya Daudi na wakapigana naye. 18 Washami
wakakimbia mbele ya Israeli. Daudi akaua askari mia saba wa magari na askari
wa farasi elfu arobaini. Shobaki mkuu wa jeshi lao alijeruhiwa na akafa huko.
19 Wafalme wote waliokuwa watumishi wa Hadareza walipoona kuwa wameshindwa
na Israeli, walifanya amani na Israeli na wakawa watumishi wao. Hivyo washami
wakaogopa kuwasaidia watu wa Amoni tena.

# 11

1 Ikawa wakati wa majira ya kipupwe, wakati ambapo kwa kawaida wafalme
huenda vitani, Daudi akamtuma Yoabu, mtumishi wake, na jeshi lote la Israeli.
Wakaliaribu jeshi la Amoni na kuuhusuru Raba. Lakini Daudi akakaa Yerusalemu.
2 Hivyo ikawa siku moja wakati wa jioni Daudi akaamka kutoka kitandani na
akatembea katika dari la kasri. Akiwa pale akamwona mwanamke aliyekuwa akioga,
mwanamke yule alikuwa mzuri sana kwa mwonekano. 3 Hivyo Daudi akatuma na
kuuliza watu waliomfahamu yule mwanamke. Mtu mmoja akasema, “Je huyu siye
Bathsheba, binti Eliamu, naye si mke wa Uria mhiti? 4 Daudi akatuma wajumbe
nao wakamchukua; akaja kwake, na akalala naye(kwani ndo alikuwa amejitakasa
kutoka siku zake). Kisha akarudi nyumbani kwake. 5 Mwanamke akawa mjamzito,
naye akatuma na kumwambia Daudi; akasema, “mimi ni mjamzito.” 6 Kisha Daudi
akatuma watu kwa Yoabu kusema, “Umtume kwangu Uria mhiti.” Hivyo Yoabu
akamtuma Uria kwa Daudi. 7 Uria alipofika, Daudi akamuuliza hali ya Yoabu.
Jinsi jeshi lilivyokuwa likiendelea, na jinsi vita vilivyokuwa vinaendelea. 8 Daudi
akamwambia Uria, “Shuka nyumbani kwako, unawe miguu yako. “Hivyo Uria
akaondoka katika kasri la mfalme, mfalme akamtumia zawadi kwa Uria. 9 Lakini
Uria akalala pamoja na watumishi wa bwana wake katika lango la kasri, wala
hakushuka nyumbani kwake. 10 Daudi alipoambiwa, “Uria hakushuka nyumbani
kwake,” akamwambia Uria, Je haukutoka safarini? Kwa nini haukushuka nyumbani
kwako?” 11 Uria akamjibu Daudi, “Sanduku, na Israeli na Yuda wamo kwenye
mahema, na Yoabu na watumishi wa bwana wangu wamepiga hema uwandani. Jinsi
gani basi mimi naweza kwenda nyumbani kwangu kula kunywa na kulala na mke
wangu? kwa hakika kama uishivyo, sitafanya hivyo. 12 Hivyo Daudi akamwambia
Uria, “Ukae leo pia, kesho nitakuacha uende.” Kwa hiyo uria akakaa Yerusalemu
siku hiyo na iliyofuata. 13 Daudi alipomwita, alikula na kunywa pamoja naye, Daudi
akamfanya alewe. Wakati wa jioni Uria akaenda kulala kitandani pake pamoja
na watumish wa bwana wake; hakushuka nyumbani kwake. 14 Hivyo asubuhi

Daudi akamwandikia Yoabu barua, naye akaituma kwa mkono wa Uria. [15] Ndani
ya barua Daudi aliandika hivi, “Mweke Uria mbele ya vita vikali sana, na kisha,
mmwache, ili apigwe na afe. [16] Hivyo Yoabu alipoona mji ukizingirwa, alimweka Uria
katika sehemu aliyojua askari adui wenye nguvu wangekuwa wakipigana. [17] Wakati
watu wa mji walipotoka na kupigana dhidi ya jeshi la Yoabu, baadhi ya askari wa
Daudi wakaanguka, na Uria Mhiti pia akauwawa. [18] Wakati Yoabu alipotuma neno
kwa mfalme kuhusu hali ya vita, [19] alimwagiza mjumbe, kusema, “Utakapomaliza
kumwambia mfalme kuhusu hali ya vita, [20] yawezekana mfalme akakasirika, naye
akakwambia, 'Kwa nini mlipigana na mji kwa karibu hivyo, hamkujua kwamba
wangeweza kushambulia kutokea ukutani? [21] Ni nani aliyemwua Abimeleki mwana
wa Yerubeshethi? Siye mwanamke aliyerusha jiwe la kusagia juu yake kutoka
ukutani, hata akafa huko Thebesi? Kwanini basi mliukaribia ukuta jinsi hiyo? Nawe
umjibu, 'Uria mtumishi wako amekufa pia.” [22] Hivyo mjumbe akaondoka na kwenda
kwa Daudi akamwambia kila jambo ambalo Yoabu alimtuma kusema. [23] Na mjumbe
akamwambia Daudi, “Mwanzoni adui walikuwa na nguvu kuliko sisi; walitukabili
uwandani, lakini tukawarudisha nyuma kwenye maingilio ya lango. [24] Na wapiga
mishale wao wakawarushia watumishi wako kutoka ukutani, na baadhi ya watumishi
wa mfalme wameuawa, na mtumishi wako Uria mhiti pia ameuawa.” [25] Kisha Daudi
akamwambia mjumbe, “Mwambie hivi Yoabu, 'Usiruhusu jamba hili likuhuzunishe,
kwa maana upanga huangamiza huyu kama uangamizavyo na mwingine. Vifanye
vita vyako kuwa vyenye nguvu zaidi dhidi ya mji, na uuteke.' Mtie moyo Yoabu.”
[26] Hivyo mke Uria aliposikia kwamba mme wake amekufa, akaomboleza sana kwa
ajili yake. [27] Huzuni yake ilipoisha, Daudi akatuma na kumchukua kwake katika
kasri lake, naye akawa mkewe na akamzalia mwana. Lakini alichokifanya Daudi
hakikumpendeza Yahwe.

# 12

[1] Kisha Yahwe akamtuma Nathani kwa Daudi. Akaja kwake na kusema, “Kulikuwa
na watu wawili katika mji. Mmoja alikuwa tajiri na mwingine alikuwa masikini.
[2] Yule tajiri alikuwa na kundi la ng'ombe na kondoo wengi sana, [3] lakini maskini
hakuwa na chochote isipokuwa mwanakondoo, aliyekuwa amemnunua na kumlisha
na kumlea. Akakua pamoja naye na pamoja na watoto wake. Yule mwanakondoo
hata alikula naye na kunywa kutoka katika kikombe chake, naye akalala katika
mikono yake na alikuwa kama binti kwake. [4] Siku moja tajiri akapata mgeni, lakini
yeye hakuwa tiyari kuchukua mnyama kutoka katika kundi lake la ng'ombe au
kundi la kondoo ili kumwandalia chakula. Badala yake alichukua mwanakondoo
wa masikini na akampika kwa ajili ya mgeni wake. [5] Hasira ya Daudi ikawaka dhidi
ya tajiri yule, naye akamwambia Nathani kwa hasira, “Kama Yahwe aishivyo, mtu
aliyelitenda jambo hili anastahili kufa. [6] Ni lazima alipe mwanakondoo mara nne
zaidi kwa ajili ya kile alichokifanya, na kwa sababu hakuwa na huruma kwa mtu
maskini. [7] Ndipo Nathani akamwambia Daudi, “Wewe ndiye yule mtu! Yahweh,
Mungu wa Israeli, asema, 'Nilikutia mafuta uwe mfalme juu ya Israeli, na nilikuokoa
kutoka katika mkono wa Sauli. [8] Nikakupa nyumba ya bwana wako, na wake
zake mikononi mwako. Nilikupa pia nyumba ya Israeli na Yuda. Na ikiwa hayo
yalikuwa kidogo zaidi kwako, ningeweza kukuongezea mengine zaidi. [9] Hivyo basi
kwa nini umedharau maagizo ya Yahwe, hata ukafanya yaliyo maovu mbele zake?
Umeua Uria Mhiti kwa upanga na umechukua mkewe kuwa mke wako. Uliua kwa
upanga wa jeshi la Amoni. [10] Hivyo basi upanga hautaondoka nyumbani mwako,
kwa kuwa umenidharau na umemchukua mke wa Uria mhiti kuwa mke wako.'
[11] Yahwe asema, 'Tazama, nitaleta maafa dhidi yako kutoka katika nyumba yako

mwenyewe. Nitachukua wake zako, mbele ya macho yako na kumpa jirani yako,
naye atalala na wake zako wakati wa mchana. 12 Kwa maana wewe ulitenda dhambi
hii sirini, lakini mimi nitatenda jambo hili wakati wa mchana mbele za Israeli wote.
13 Ndipo Daudi alipomwambia Nathani, “Nimemtenda dhambi Yahwe.” Nathani
akamjibu Daudi, “Yahwe naye ameiachilia dhambi yako. Hautakufa. 14 Lakini, kwa
kuwa kwa tendo hili umemdharau Yahwe, mtoto aliyezaliwa kwako hakika atakufa.”
15 Kisha Nathani akaondoka na kwenda kwake. Yahwe akampiga mtoto ambaye
mke wa Uria alimzaa kwa Daudi, naye akaugua sana. 16 Kisha Daudi akamwomba
Mungu kwa ajili ya kijana. Daudi akafunga naye akaingia ndani na kulala usiku
wote juu ya sakafu. 17 Wazee wa nyumba yake wakainuka na kusimama kando
yake, ili wamwinue kutoka sakafuni. Lakini hakuinuka, na hakula pamoja nao.
18 Ikawa siku ya saba mtoto akafa. Watumishi wa Daudi wakaogopa kumwambia
kwamba mtoto amekufa, kwa maana walisema, “Tazama, wakati mtoto alipokuwa
hai tuliongea naye, lakini hakuisikiliza sauti yetu. Atakuwaje ikiwa tutamwambia
kwamba kijana amekufa?!” 19 Daudi alipoona kwamba watumishi wake walikuwa
wakinong'onezana, Akatambua kwamba mtoto amekufa. Akawauliza, “Je mtoto
amekufa?” Wakajibu, “Amekufa.” 20 Kisha Daudi akainuka kutoka sakafuni naye
akaoga, akajipaka mafuta, na kubadili mavazi yake. Akaenda katika hema la
kukutania na akaabudu pale, kisha akarudu katika kasri lake. Akataka chakula
kiletwe, wakamwandalia, naye akala. 21 Ndipo watumishi wake walipomwambia,
“Kwa nini umefanya jambo hili? Ulifunga na kulia kwa ajili ya mtoto wakati
alipokuwa hai, lakini mtoto alipokufa, ukainuka na kula.” 22 Daudi akajibu, “Wakati
mtoto alipokuwa hai nilifunga na kulia. Nilisema, Ni nani ajuaye kwamba Yahwe
angeweza kunihurumia mtoto akaishi au sivyo? 23 Lakini sasa amekufa, hivyo
nifungie nini? Je naweza kumrudisha tena? Nitakwenda kwake, lakini yeye hawezi
kunirudia.” 24 Daudi akamfariji Bethsheba mkewe, akaingia kwake, na akalala naye.
Baadaye akazaa mtoto wa kiume, naye akaitwa Selemani. Yahwe akampenda 25 naye
akatuma neno kupitia nabii Nathani kumwita Yedidia, kwa sababu Yahwe alimpenda.
26 Basi Yoabu akapigana na Raba, mji wa kifalme wa watu wa Amoni, naye akaiteka
ngome yake. 27 Hivyo Yoabu akatuma wajumbe kwa Daudi na kusema, “Nimepigana
na Raba, nami nimeshikilia sehemu inayosambaza maji ya mji. 28 Kwa hiyo sasa
likusanye jeshi lililosalia uhuzingire mji na kuuteka, kwa maana ikiwa nitauteka,
utaitwa kwa jina langu.” 29 Hivyo Daudi akalikusanya jeshi lote na kwenda Raba;
akapigana nao na kuuteka. 30 Daudi akachukua taji ya dhahabu kutoka katika kichwa
cha mfalme wao iliyokuwa na uzito wa talanta, na ilikuwa na jiwe la thamani ndani
yake. Taji ikawekwa juu ya kichwa cha Daudi. Kisha akachukua nyara za mji kwa
wingi. 31 Akawatoa watu waliokuwa mjini naye akawalazimisha kufanya kazi kwa
misumeno, sululu na shoka; lakini pia akawalazimisha kutengeneza matofali. Daudi
akailazimisha miji yote ya watu wa Amoni kufanya kazi hiyo. Kisha Daudi na jeshi
lote wakarudi Yerusalemu

# 13

1 Ikawa baada ya hayo kwamba Amnoni mwana wa Daudi, akamtamani sana
Tamari dada yake wa kambo aliyekuwa mzuri, alikuwa tumbo moja na Absalome,
mwana wingine wa Daudi. 2 Amnoni akasononeka sana kiasi cha kuugua kwa
ajili ya Tamari dada yake. Tamari alikuwa bikra, na hivyo ilionekana haiwezekani
Amnoni kufanya neno lolote kwake. 3 Lakini Amnoni alikuwa na rafiki jina lake
Yehonadabu mwana wa Shama, nduguye Daudi. 4 Yehonadabu alikuwa mtu mwelevu
sana. Akamwambia Amnoni, “Kwa nini, mwana wa mfalme, unadhoofika kila
siku? Kwa nini uniambii? Ndipo Amnoni akamjibu, “Nampenda Tamari, dada

yake Absalome ndugu yangu." [5] Ndipo Yehonadabu akamwambia, "Lala kitandani
mwako na ujifanye kuwa mgonjwa. Wakati baba yako atakapo kuja kukuona,
mwambie, Tafadhari mtume dada yangu Tamari aandaye chakula mbele yangu,
ili kwamba nikione na kula kutoka mkononi mwake?" [6] Hivyo Amnoni akalala
na kujifanya kuwa mgonjwa. Mfalme alipokuja kumwona, Amnoni akamwambia
mfalme, "Tafadhari mtume Tamari dada yangu aandaye chakula kwa ajili ya ugonjwa
wangu mbele yangu ili kwamba nikile kutoka mkononi mwake. [7] Ndipo Daudi
katika kasri lake akatuma neno kwa Tamari, kusema, "Nenda katika nyumba ya
nduguyo Amnoni na umwandalie chakula. Hivyo [8] Tamari akaenda katika nyumba
ya Amnoni nduguye alipokuwa amelala. Akachukua donge na kulifinyanga na
kuandaa mkate mbele zake, kisha akauoka. [9] Akachukua kikaangio na kumpa
mkate, lakini akakataa kula. Kisha Amnoni akawambia waliokuwepo, "Kila mtu
na aondoke." Hivyo kila mmoja akaondoka. [10] Amnoni akamwambia Tamari,
"Lete chakula chumbani kwangu nikile katika mkono wako." Tamari akachukua
mkate aliokuwa ameuandaa, na kuuleta katika chumba cha Amnoni kaka yake.
[11] Alipoleta chakula kwake, Amnoni akamshikilia na kumwambia, "Njoo, ulale nami,
dada yangu." [12] Yeye akamjibu, "Hapana, kaka yangu, usinilazimishe, kwani hakuna
jambo kama hili linapaswa kufanyika katika Israeli. Usifanye jambo la aibu kiasi
hiki! [13] Nitakwenda wapi ili nijiepushe na aibu ambayo jambo hili litaileta juu ya
maisha yangu? Na tendo hili litakuonesha kuwa mpumbavu usiye na aibu katika
Israeli yote. Tafadhari, ninakuomba uongee na mfalme. Yeye atakuruhusu unioe."
[14] Lakini Amnoni hakuweza kumsikiliza. Kwa kuwa alikuwa zaidi akamkamata na
akalala naye. [15] Kisha Amnoni akamchukia Tamari kwa chuki kuu. Akamchukia
zaidi ya jinsi alivyokuwa amemtamani. Amnoni akamwambia, "Inuka na uondoke."
[16] Lakini yeye akamjibu, "Hapana! kwa maana uovu wa kunifanya ni uondoke ni
mbaya zaidi ya kile ulichonitenda!" Lakini Amnoni hakumsikiliza. [17] Badala yake,
akamwita mtumishi wake na akasema, "Mwondoe mwanamke huyu mbele yangu,
na uufunge mlango nyuma yake." [18] Hivyo mtumishi wake akamtoa na kufunga
mlango. Tamari alikuwa amevaa vazi lilinakishiwa kwani ndivyo binti za wafalme
waliobikra valivyokuwa wakivaa. [19] Tamari akaweka majivu juu ya kichwa chake
na akalirarua vazi lake [20] Absalome, kaka yake, akamwambia, "Amnoni, kaka yako,
amekuwa nawe? Lakini sasa nyamaza, dada yangu. Yeye ni kaka yako. Usiliweke
hili moyoni." Hivyo Tamari akakaa peke yake katika nyumba ya Absalomu kaka
yake. [21] Mfalme Daudi aliposikia haya yote, alikasirika sana. [22] Absalome hakusema
chochote kwa Amnoni, kwa maana Absalome alimchukia kwa kile alichokifanya,
kumdhalilisha Tamari, dada yake. [23] Ikawa baada ya miaka miwili mizima Absalomu
akawa na wakatao kondoo manyoya wakifanya kazi huko Baali Hazori, ulioko
karibu na Efraim, naye Absalomu akawaarika wana wote wa mfalme kufika huko.
[24] Absalomu akamwendea mfalme na kusema, "Tazama sasa, mtumishi wako anao
wakatao kondoo manyoya. Tafadhari, naomba mfalme na watumishi wake waende
nami, mtumishi wako." [25] Mfalme akamjibu Absalomu, "hapana mwanangu, tusiende
sisi yote kwani tutakuwa mzigo kwako." Absalomu akamhakikishia mfalme, lakini
yeye asikubali kwenda, ila alimbariki Absalomu. [26] Kisha Absalomu akasema, "kama
sivyo, basi tafadhari mwache ndugu yangu Amnoni aende nasi." Mfalme akamuliza,
"Kwa nini Amnoni aende nanyi?" [27] Absalomu akamsihi Daudi, hivyo akamruhusu
Amnoni na wana wengine wa mfalme kwenda naye. [28] Absalomu akawaamuru
watumishi wake kusema, "Sikilizeni kwa makini. Amnoni atakapokuwa amelewa
mvinyo, na nitakapowambia, 'Mpigeni Amnoni,' msiogope mwueni. Je siyo mimi
niliyewamru? Mwe jasiri na hodari." [29] Hivyo watumishi wa Absalome wakamtendea
Amnoni kama walivyoamriwa. Kisha wana wote wa mfalme wakainuka na kila

mmoja akapanda nyumbu wake akakimbia. [30] Hata ikawa wakati wakiwa njiani
habari zikafika kwa Daudi kusema, “Absalomu ameua wana wote wa mfalme na
hakuna hata mmoja aliyesalia.” [31] Kisha mfalme akainuka na kurarua mavazi
yake na kujilaza juu ya sakafu; watumishi wake wote wakasimama karibu naye
mavazi yao yameraruriwa. [32] Yehonadabu mwana wa Shama, nduguye Daudi,
akajibu na kusema, “Bwana wangu asidhani kuwa vijana wote ambao ni wana
wa mfalme wameuawa, kwa maana ni Amnoni pekee ndiye aliyeuawa. Absalomu
alilipanga jambo hili tangu siku ile Amnoni alivyomwaribu Tamari, dada yake.
[33] Kwa hiyo basi, bwana wangu mfalme asiiweke taarifa hii moyoni, kudhani
kwamba wana wote wa mfalme wameuawa, kwani aliyeuawa ni Amnoni peke yake.”
[34] Absalomu akakimbia. Mtumishi aliyekuwa akiangalia akainua macho yake na
kuona watu wengi wakija njiani kando ya kilima upande wake wa magharibi. [35] Kisha
Yehonadabu akamwambia mfalme, “Tazama, wana wa mfalme wanakuja. kama
mtumishi wako alivyosema.” [36] Ikawa mara alipomaliza kusema wana wa mfalme
wakafika, wakainua sauti zao na kulia. Na mfalme pamoja na watumishi wake wote
pia wakalia kwa uchungu. [37] Lakini Absalomu akakimbia na kwenda kwa Talmai
mwana wa Amihudi, mfalme wa Geshuri. Mfalme akaomboleza kila siku kwa ajili ya
mwanaye. [38] Hivyo Absalomu akakimbia na kwenda Geshuri na akakaa huko kwa
miaka mitatu. [39] Moyo wa mfalme Daudi ukatamani kwenda kumwona Absalomu,
kwa maana alikuwa amefarijika kwa habari ya kifo cha Amnoni.

# 14

[1] Yoabu mwana wa Seruya akatambua kwamba moyo wa mfalme ulitamani
kumwona Absalomu. [2] Hivyo Yoabu akatuma neno huko Tekoa kumleta kwake
mwanamke mwelevu. Akamwambia, “Tafadhari, vaa mavazi ya uombolezaji uji-
fanye kuwa mwombolezaji. Usijipake mafuta, lakini uwe kama mwanamke ambaye
ameomboleza kwa muda mrefu kwa ajili yake aliyekufa. [3] Kisha ingia kwa mfalme na
umwambiye maneno nitakayokueleza.” Hivyo Yoabu akamwambia maneno ambayo
angeyasema kwa mfalme. [4] Wakati mwanamke kutoka Tekoa alipoongea na mfalme,
aliinamisha uso wake chini na kusema, [5] “Mfalme, anisaidie.” Mfalme akamwambia,
“Shida yako ni nini?” Akajibu, Ukweli ni kwamba mimi ni mjane, mme wangu
alikufa. [6] Mimi, mtumishi wako, nilikuwa na wana wawili, wakagombana shambani,
na hakukuwa na wa kuwaachanisha. Mmoja wao akampiga mwenziwe na kumwua.
[7] Na sasa ukoo wote umeinuka juu ya mtumishi wako, wanasema, 'Mtoe aliyempiga
nduguye, ili tumwue kulipe uhai wa nduguye aliyeuawa.' Na hivyo watamwangamiza
mrithi. Hivyo watalizima kaa liwakalo nililobakiwa, hata kumwondolea mme wangu
jina na mzao juu ya uso wa nchi.” [8] Hivyo mfalme akamwambia mwanamke,
“Nenda nyumbani kwako, nami nitaagiza jambo la kukufanyia.” [9] Mwanamke kutoka
Tekoa akamjibu mfalme, “Bwana wangu mfalme, hatia na iwe juu yangu na juu ya
familia ya baba yangu. Mfalme na kiti chake cha enzi hawana hatia.” [10] Mfalme
akasema, “Yeyote atakayekwambia neno umlete kwangu, naye hatakugusa tena.”
[11] Kisha mwanamke akasema, “Tafadhari mfalme amkumbuke Yahwe Mungu wake,
ili kwamba mlipa kisasi cha damu asiaribu zaidi, ili kwamba wasimwangamize
mwanangu.” Mfalme akajibu, “Kama Mungu aishivyo, hakuna hata unywele mmoja
wa mwanao utaanguka chini.” [12] Kisha mwanamke akasema, “Tafadhari acha
mtumishi wako anene neno moja zaidi kwa bwana wangu mfalme.” Akasema,
“Sema.” [13] Hivyo mwanamke akasema, “Kwa nini basi umetenda kwa hila dhidi
ya watu Mungu? Maana kwa kusema hivi, mfalme ni kama mtu mwenye hatia,
kwa kuwa mfalme hamjamrudisha tena mwanaye aliyeondoka. [14] Kwa maana sisi
sote tutakufa, kwa kuwa tu kama maji yamwagwayo juu ya ardhi na kwamba

hayawezi kukusanywa tena. Lakini Mungu hatachukua uhai; badala yake, utafuta
njia kwa walio mbali kurejeshwa. [15] Sasa basi, nimesema jambo hili kwa bwana
wangu mfalme, kwa sababu watu wamenitisha. Hivyo mtumishi wako akajinenea
nafsini mwake, 'Sasa nitaongea na mfalme. Huenda mfalme akampa mtumishi wake
haja yake. [16] Kwa maana mfalme atanisikiliza, ili kwamba kumtoa mtumishi wake
katika mikono ya mtu ambaye angeniangamiza mimi na mwanangu pamoja, tutoke
katika urithi wa Mungu. [17] Kisha mtumishi wako akaomba, 'Yahwe, tafadhari ruhusu
neno la bwana wangu mfalme linipe msaada, kwa maana bwana wangu mfalme ni
kama malaika wa Mungu kwa kutofautisha wema na ubaya.' Yahwe, Mungu na awe
pamoja nawe." [18] Ndipo mfalme akajibu na kumwambia yule mwanamke, Tafadhari
usinifiche neno lolote nikuulizalo." Mwanamke akajibu, "Basi bwana wangu mfalme
na aseme sasa. [19] Mfalme akasema, Je siyo mkono wa Yoabu ulio pamoja nawe katika
haya yote? Mwanamke akajibu na kusema, "Kama uishivyo bwana wangu mfalme,
hakuna awezae kuelekea mkono wa kulia wala wa kushoto kwa yale bwana wangu
mfalme aliyosema. Ni mtumishi wako Yoabu aliyeniambia na kuniagiza kusema kile
mtumishi wako alichokisema. [20] Mtumishi wako Yoabu amefanya hivi ili kubadilisha
hali ya kile kinachotendeka. Bwana wangu ni mwenye akili kama hekima ya malaika
wa Mungu, ajuaye yote yatendekayo ndani ya nchi." [21] Hivyo mfalme akamwambia
Yoabu, "Tazama, nitatenda jambo hili. Nenda na umrudishe huyo kijana Absalomu."
[22] HivyoYoabu akainamisha uso wake chini juu ya ardhi katika heshima na shukurani
kwa mfalme. Yoabu akasema, "Mtumishi wako amejua kwamba amepata neema
mbele zako, bwana wangu, mfalme, kwa vile mfalme amempa mtumishi wake haja
ya moyo wake. [23] Hivyo Yoabu akainuka na kwenda Geshuri, akamrejesha Absalomu
Yerusalemu tena. [24] Mfalme akasema, "Na arudi nyumbani kwake, lakini hasinione
uso wangu." Hivyo Absalomu akarudi katika nyumba yake mwenyewe, na hakuweza
kuuona uso wa mfalme. [25] Hakukuwa na mtu katika Israeli aliyesifiwa kwa uzuri
kama Absalomu. Kutoka katika wayo wa mguu wake hadi katika utosi wake hakuwa
na waa lolote. [26] Alipokata nywele za kichwa chake mwishoni mwa kila mwaka,
kwa sababu zilikuwa nzito juu yake, alipima nywele zake zaidi ya shekeli mia mbili,
kwa kiwango cha kipimo cha mfalme. [27] Kwake Absalomu walizaliwa wana watatu
na binti mmoja, jina lake Tamari. Alikuwa mwanamke mzuri. [28] Absalomu akaishi
Yerusalem miaka miwili pasipo kuona uso wa mfalme. [29] Kisha Absalome akatuma
neno kwa Yoabu ili ampeleke kwa mfalme, lakini Yoabu hakwenda kwake. Hivyo
Absalomu akatuma neno mara ya pili, lakini Yoabu hakuja bado. [30] Hivyo Absalomu
akawambia watumishi wake, "Tazameni, shamba la Yoabu lipo karibu na langu,
naye ana shayiri kule. Nendeni mkalichome moto" Hivyo watumishi wa Absalome
wakalichoma moto lile shamba. [31] Kisha Yoabu akainuka na kwenda nyumbani kwa
Absalomu akamwambia, "Kwa nini watumishi wako wamelichoma moto shamba
langu? [32] Absalomu akamjibu Yoabu, "Tazama nilituma neno kwako kusema, 'Njoo
ili nikutume kwa mfalme kusema, "Kwa nini nilikuja kutoka Geshuri? Ingekuwa
heri kwangu kama ningesalia huko. Kwa hiyo sasa niache niuone uso wa mfalme na
kama nina hatia basi na aniue." [33] Hivyo Yoabu akaenda kwa mfalme na kumwambia.
Mfalme alipomwita, Absalomu alikuja kwa mfalme na akainama hadi juu ya uso nchi
mbele ya mfalme na mfalme akambusu Absalomu.

# 15

[1] Ikawa baada ya haya Absalomu akaandaa gari la farasi na farasi kwa ajili yake
pamoja na watu hamsini wa kwenda mbele zake. [2] Absalomu alikuwa akiamka
mapema na kusimama kando ya njia iliyoelekea katika lango la mji. Mtu yeyote
aliyekuwa na shauri la kuja kwa mfalme kwa ajili ya hukumu, Absalomu alimwita

na kumwuliza, "Unatoka mji upi?" Na mtu yule hujibu, Mtumishi wako anatoka
mojawapo ya kabila za Israeli." 3 Hivyo Absalomu umwambia, "Tazama, shitaka lako
ni jema na la haki, lakini hakuna aliyepewa mamlaka na mfalme kusikiliza shitaka
lako. 4 Absalomu uongeza, "Natamani kwamba ningefanywa mwamzi ndani ya nchi
ili kwamba kila mtu aliye na shitaka angeweza kuja kwangu nami ningempa haki.
5 Hivyo ikawa kila mtu aliyekuja kumweshimu Absalomu yeye hunyosha mkono na
kumshika na kumbusu. 6 Absalomu alifanya hivi kwa Israeli wote waliokuja kwa
mfalme kwa ajili ya hukumu. Hivyo Absalomu akaipotosha mioyo ya watu wa Israeli.
7 Ikawa mwishoni mwa miaka minne Absalomu akamwambia mfalme, "Tafadhari
niruhusu niende ili nitimize nadhiri niliyoiweka kwa Yahwe huko Hebroni. 8 Kwa
maana mtumishi wako aliweka nadhiri alipokuwako Geshuri katika Shamu akisema,
'Ikiwa Yahwe kweli atanirejesha Yerusalemu, ndipo nitamwabudu yeye." 9 Hivyo
mfalme akamwambia, "Nenda kwa amani". Absalomu akainuka na kwenda Hebroni.
10 Kisha Absalomu akatuma wapelelezi katika jamaa zote za Israeli, kusema, "Mara
msikiapo sauti ya tarumbeta semeni, 'Absalomu anatawala katika Hebroni." 11 Watu
mia mbili waliokuwa wamearikwa kutoka Yerusalemu wakaenda na Absalomu.
Wakaenda katika ujinga wao bila kujua Absalomu alichokipanga. Wakati 12 Absalomu
akitoa dhabihu, alituma watu kwa Ahithofeli katika mji wake huko Gilo. Yeye alikuwa
mshauri wa Daudi. Uaini wa Absalomu ukawa na nguvu kwa kuwa watu waliomfuata
waliendelea kuongezeka. 13 Mjumbe akaja kwa Daudi na kusema, "Mioyo ya watu
wa Israeli inaambatana na Absalomu." 14 Hivyo Daudi akawambia watumishi wake
waliokuwa pamoja naye huko Yerusalemu, "Haya na tuinuke na kukimbia kwani
hakuna hata mmoja atakayesalimika kwa Absalomu. Jiandaeni kuondoka mara moja
asije akatupata mara hata akasababisha madhara juu yetu na kuushambulia mji kwa
makali ya upanga." 15 Watumishi wa mfalme wakamwambia, "Tazama, watumishi
wako wapo tiyari kufanya lolote bwana wetu mfalme atakaloamua. 16 Mfalme
akaondoka na familia yake yote pamoja naye, lakini mfalme akawaacha wanawake
kumi waliokuwa masuria wa mfalme ili walitunze kasri. 17 Baada ya mfalme kwenda
na watu wote pamoja naye, wakasimama katika nyumba ya mwisho. 18 Jeshi lake lote
likaenda pamoja naye na mbele yake wakaenda Wakerethi na Wapelethi, na Wagiti
mia sita wote waliokuwa wamemfuata kutoka Gathi. 19 Kisha mfalme akamwambia
Itai Mgiti, "Kwa nini wewe pia uende nasi? Rudi na ukae na mfalme Absalomu kwa
kuwa wewe ni mgeni tena mfungwa. Rudi mahali pako mwenyewe. 20 Kwani ni
jana tu umeondoka, kwa nini nikufanye uzunguke nasi popote? Hata sijui niendako.
Hivyo rudi pamoja na wenzako. Utiifu na uaminifu viambatane nawe." 21 Lakini Itai
akamjibu mfalme na kusema, "Kama Yahwe aishivyo na kama bwana wangu mfalme
aishivyo, kwa hakika mahali popote bwana wangu mfalme aendako, mtumishi wako
pia ndipo atakapokwenda, kwamba ni maisha au kifo." 22 Hivyo Daudi akamwambia
Itai, haya tangulia uende pamoja nasi." Hivyo Itai Mgiti akaenda pamoja na mfalme,
pamoja na watu wake wote na familia zao zote. 23 Nchi yote ikalia kwa sauti kadili
watu walivyokuwa wakivuka Bonde la Kidroni, mfalme naye pia akavuka. Watu
wote wakasafiri kuelekea nyikani. 24 Walikuwepo pia Sadoki pamoja na Walawi
wote wamebeba sanduku la Mungu la agano. Wakaliweka sanduku la Mungu chini
na kisha Abiathari akaungana nao. Wakasubiri mpaka watu wote walioondoka mjini
walipokwisha kupita. 25 Mfalme akamwambia Sadoki, "Ulirudishe sanduku la Mungu
mjini. Ikiwa nitaona neema machoni pa Yahwe atanirudisha na kunionesha tena
sanduku na mahali likaapo. 26 Lakini ikiwa atasema, sipendezwi nawe,' tazama mimi
nipo hapa, na anitendee yaliyo mema machoni pake." 27 Pia mfalme akamwambia
Sadoki kuhani, "Je wewe siyo mwonaji? Rudi mjini kwa amani na wanao wawili,
Ahimaazi mwanao na Yonathani mwana wa Abiathari. 28 Tazama nitasubiri katika

vivuko vya Araba mpaka nitakapo pata neno kutoka kwenu kunitaarifu.” 29 Hivyo
Sadoki na Abiathari wakalirudish sanduku la Mungu Yerusalemu nao wakakaa
humo. 30 Lakini Daudi akaenda bila viatu huku akilia hata Mlima wa Mizeituni,
naye alikuwa amefunika kichwa chake. Kila mtu miongoni mwao waliokuwa
pamoja naye akafunika kichwa chake, nao wakaenda huku wakilia. 31 Mtu mmoja
akamwambia Daudi kusema, Ahithofeli ni miongoni mwa waaini walio pamoja na
Absalomu.” Hivyo Daudi akaomba, “Ee Yahwe, tafadhari badili ushauri wa Ahithofeli
kuwa upumbavu.” 32 Ikawa Daudi alipofika juu njiani mahala Mungu alipokuwa
akiabudiwa, Hushai Mwarki akaja kumlaki vazi lake limeraruliwa na mavumbi
kichwani pake. 33 Daudi akamwambia, “Ikiwa utaenda nami utakuwa mzigo kwangu.
34 Lakini ukirudi mjini na kumwambia Absalomu, 'Nitakuwa mtumishi wa mfalme
kama nilivokuwa mtumishi wa baba yako, ndivyo nitakavyokuwa mtumishi wako,'
ndipo utayageuza mashauri ya Ahithofeli kwa ajili yangu. 35 Je haunao pamoja nawe
Sadoki na Abiathari makuhani? Hivyo chochote ukisikiacho katika kasri, uwaambie
Sadoki na Abiathari makuhani. 36 Tazama wanao pamoja nao wana wao wawili,
Ahimaasi, mwana wa Sadoki, na Yonathani mwana wa Abiathari. Mniletee habari
juu ya kila mnachokisikia.” 37 Hivyo Hushai, rafiki wa Daudi, akaja mjini wakati
Absalomu anafika na kuingia Yerusalemu.

# 16

1 Daudi alipokuwa amekwenda kitambo juu ya kilele cha kilima, Siba mtumishi wa
Mefiboshethi akaja kumlaki akiwa na punda wawili waliokuwa wamebeba vipande
mia mbili vya mikate, vishada mia moja vya mizeituni, vishada mia moja vya tini
na mfuko wa ngozi uliojaa mvinyo. 2 Mfalme akamuliza Siba, “Kwa nini umeleta
hivi vitu?” Siba akajibu, “punda ni kwa ajili ya familia yako kupanda, mikate na
matunda ni kwa ajili ya matumizi ya askari wako, na mvinyo ni kwa ajili kunywa
watakaozimia nyikani.” 3 Mfalme akauliza, “Na mjukuu wa bwana wako yuko
wapi?” Siba akamjibu mfalme, “Tazama, yeye amesalia Yerusalemu kwa maana
alisema, 'Leo nyumba ya Israeli itanirudishia ufalme wa baba yangu.” 4 Kisha
mfalme akamwambia Siba, “Tazama, yote yaliyomilikiwa na Mefiboshethi sasa
yatakuwa yako.” Siba akajibu, “Nainama kwa unyenyekevu kwako bwana wangu
mfalme. Na nipate kibari mbele zako.” 5 Mfalme Daudi alipokaribia Bahurimu,
akaja mtu kutoka katika ukoo wa Sauli, jina lake Shimei mwana wa Gera. Kadiri
alivyokuwa akitembea alikuwa akilaani. 6 Akamrushia Daudi mawe na maofisa
wa mfalme, bila kujali jeshi na walinzi wa mfalme waliokuwa kulia na kushoto
mwa mfalme. 7 Shimei akalaani, “Nenda zako, toka hapa, mwovu wewe, mtu
wa damu! 8 Yahwe amelipa yote kwa ajili ya damu ya familia ya Sauli, ambaye
unatawala badala yake. Yahwe ameweka ufalme katika mkono wa Absalomu
mwanao. Na sasa umeangamia kwa kuwa ni mtu wa damu.” 9 Ndipo Abishai
mwana wa Seruya, akamwambia mfalme, “Kwa nini mbwa mfu anamlaani bwana
wangu mfalme? Tafadhari niache niende nikamwondolee kichwa chake.” 10 Lakini
mfalme akasema, “Nifanye nini nanyi enyi wana wa Seruya? Pengine ananilaani
kwa kuwa Yahwe amemwambia, 'Mlaani Daudi.' Nani sasa awezaye kumwambia,
'Kwa nini unamlaani mfalme.” 11 Hivyo Daudi akamwambia Abishai na watumishi
wake wote, “Tazameni, mwanangu aliyezaliwa kutoka katika mwili wangu anatafuta
uhai wangu. “Si zaidi sana mbenjamini huyu akatamani anguko langu? Mwacheni
alaani, kwa maana Yahwe amemwamru kufanya hivyo. 12 Huenda Yahwe akaangalia
maangaiko niliyofungiwa, na kunirudishia mema kwa jinsi nilivyolaaniwa leo.”
13 Hivyo Daudi na watu wake wakaendelea njiani wakati Shimei kando yake ubavuni
mwa mlima, aliendelea kulaani na kumrushia mavumbi na mawe huku akienda.

14 Kisha mfalme na watu wake wote wakachoka, na akapumzika wakati wa usiku
walipopumzika wote. 15 Absalomu na watu wote wa Israeli waliokuwa pamoja
naye wakaja Yerusalemu na Ahithofeli alikuwa pamoja naye. 16 Ikawa Hushai
Mwarki, rafiki yake Daudi, akaja kwa Absalomu, naye akamwambia Absalomu,
"Mfalme aishi daima! mfalme aishi daima. 17 Absalomu akamwambia Hushai,
"Je huu ndiyo utiifu wako kwa rafiki yako? Kwa nini haukwenda pamoja naye?"
18 Hushai akamwambia Absalomu, "Hapana! badala yake, yule ambaye Yahwe, watu
hawa na watu wote wa Israeli wamemchagua huyo ndiye nitakaye kuwa upande
wake na ndiye nitakaye kaa naye. 19 Kwani ni nani ninayepaswa kumtumikia? Je
sipaswi kutumika mbele za mwana? kama nilivyotumika mbele za baba yako ndivyo
nitakavyofanya mbele zako" 20 Kisha Absalomu akamwambia Ahithofeli, "Tupe
shauri lako kuhusu tunachopaswa kufanya." 21 Ahithofeli akamwambia Absalomu,
"Nenda ulale na masuria wa baba yako aliowaacha kutunza kasri, na waisraeli wote
watasikia kwamba umekuwa kitu kinachonuka kwa baba yako. Kisha mikono ya
wote walio pamoja nawe itatiwa nguvu." 22 Hivyo wakatanda hema kwa ajili ya
Absalomu juu ya kasri na Absalomu akalala na masuria wa baba yake mbele za
Israeli wote. 23 Nyakati hizo ushauri aliokuwa akitoa Ahithofeli ulikuwa ni kama
mtu anavyosikia kutoka katika kinywa cha Mungu mwenyewe. Hivyo ndivyo jinsi
ushauri wa Ahithofeli ulivyoonekana kwa Daudi na Absalomu

# 17

1 Kisha Ahithofeli akamwambia Absalomu, "Niruhusu sasa nichague watu elfu
kumi na mbili nami nitaondoka na kumfuatia Daudi usiku huu. 2 Nitampata kwa
ghafla wakati amechoka na dhaifu nami nitamstukiza kwa hofu. Watu waliopamoja
naye watakimbia nami nitamshambulia mfalme peke yake. 3 Nitawarejesha watu
wote kwako kama bibi harusi ajavyo kwa bwana wake, na watu wote watakuwa
katika amani chini yako." 4 Alichokisema Ahithofeli kikampendeza mfalme na wazee
wote wa Israeli. 5 Kisha Absalomu akasema, "Sasa mwiteni pia Hushai Mwarki
ili tusikie yeye pia anasemavyo." 6 Hushai alipofika kwa Absalomu, Absalomu
akamweleza kile ambacho Ahithofeli alikuwa amesema na kisha akamwuliza Hushai,
"Je tufanye alivyosema Ahithofeli? Ikiwa hapana, tueleze kile unachoshauri."
7 Hivyo Hushai akamwambia Absalomu, "Ushauri aliotoa Ahithofeli siyo mzuri
kwa wakati huu." 8 Hushai akaongeza, "Unamjua baba yako na kwamba watu
wake ni mashujaa na kwa sasa wanauchungu, ni kama dubu aliyenyang'anywa
watoto wake mwituni. Baba yako ni mtu wa vita; hatalala na jeshi usiku huu.
9 Tazama, kwa wakati huu pengine amejificha katika shimo fulani au mahali pengine.
Itakuwa kwamba baadhi ya watu wako watakapokuwa wameuawa mwanzoni mwa
shambulio hata kila mtu atakayesikia atasema, mauaji yamefanyika kwa askari
wanaomfuata Absalomu.' 10 Kisha hata askari jasiri zaidi ambao moyo wao ni kama
moyo wa simba, wataogopa kwa kuwa Israeli yote inajua kwamba baba yako ni mtu
mwenye nguvu na kwamba watu alionao ni wenye nguvu sana. 11 Hivyo ninashauri
kwamba Israeli wote wakutanike kwako pamoja kutoka Dani hadi Beersheba, wengi
kama mchanga ufuoni mwa bahari na kwamba wewe mwenyewe uende vitani.
12 Kisha tutampata popote atakapokuwa nasi tutamfunika kama umande uangukavyo
juu ya nchi. Hatutamwachia hata mmoja aliye hai kati ya watu wake wala yeye
mwenyewe. 13 Ikiwa ataingia ndani ya mji kisha Israeli wote tutaleta kamba juu ya
mji huo na kuukokotea mtoni, hata kusionekane hata jiwe moja dogo lililosalia."
14 Kisha Absalomu na watu wa Israeli wakasema, "Shauri la Hushai Mwarki ni
jema kuliko lile la Ahithofeli. Yahwe aliwafanya wakatae shauri jema la Ahithofeli
ili kumwangamiza Absalomu. 15 Kisha Hushai akawambia Sadoki na Abiathari

makuhani, “Ahithofeli alimshauri Absalomu na wazee wa Israeli hivi na hivi, lakini
mimi nimeshauri vinginevyo. 16 Sasa basi, nendeni haraka na mmtaarifu Daudi
kusema, 'Usipige kambi usiku huu katika vivuko vya Araba, lakini kwa namna
yoyote vukeni, tofauti na hapo mfalme atamezwa pamoja na watu wote walio pamoja
naye.” 17 Yonathani na Ahimaasi walikuwako katika chemichemi za En Rogeli. Hivyo
kijakazi mmoja alikuwa akienda na kuwapasha habari waliyopaswa kuifahamu, ili
kwamba wasihatarishe maisha yao kwa kuonwa wakiingia mjini. Ujumbe ulipofika
ndipo huenda na kumtaarifu mfalme Daudi. 18 Lakini kijana mmoja akawaoni mara
akamwambia Absalomu. Hivyo Yonathani na Ahimaasi wakaenda kwa haraka na
wakaingia katika nyumba ya mtu mmoja huko Bahurimu, aliyekuwa na kisima katika
ua wake wakaingia humo. 19 Mke wa mtu huyo akachukua kifuniko na kukikufunika
kwenye mlango wa kisima kisha akaanika nafaka juu yake, hivyo hakuna aliyejua
kwamba Yonathani na Ahimaasi walikuwa kisimani. 20 Watu wa Absalomu wakaja
kwa mwanamke na kumwuliza, “Ahimaasi na Yonathani wako wapi?” Mwanamke
akawaambia, “Wamevuka mto.” Hivyo baada ya kuwatafuta bila kuwaona kurejea
Yerusalemu. 21 Ikawa baada yao kuondoka Yonathani na Ahimaasi wakatoka ndani ya
kisima. Wakaenda kumtaarifu mfalme Daudi; wakamwambia, “Inuka na uvuke maji
haraka kwa maana Ahithofeli ametoa mashauri haya na haya juu yako.” 22 Kisha
Daudi akainuka pamoja na watu wote walikuwa pamoja naye, nao wakauvuka
Yordani. Hata ilipofika alfajiri hakuna hata mmoja aliyesalia kwa kutouvuka Yordani.
23 Ikawa Ahithofeli alipoona kwamba ushauri wake haukufuatwa, akapanda punda
wake na kuondoka. Akaenda nyumbani katika mji wake mwenyewe, akaweka
mambo yake katika utaratibu na kisha akajinyonga. Kwa hiyo akafa na kuzikwa
katika kaburi la baba yake. 24 Ndipo Daudi akaja Mahanaimu. Lakini Absalomu
yeye akavuka Yordani yeye pamoja na watu wote wa Israeli waliokuwa pamoja
naye. 25 Absalomu alikuwa amemweka Amasa juu ya jeshi badala ya Yoabu. Naye
huyo Amasa alikuwa mwana wa Yetheri Mwishmaeli, aliyekuwa amelala na Abigaili,
aliyekuwa binti Nahashi na dada wa Seruya, mamaye Yoabu. 26 Kisha Israeli na
Absalomu wakapiga kambi katika nchi ya Gileadi. 27 Ikawa wakati Daudi alipokuwa
amekuja Mahanaimu, huyo Shobi mwana wa Nahashi kutoka Raba ya Waamoni na
Makiri mwana wa Amieli wa kutoka Lo Debari, na Berzilai Mgileadi wa Rogelimu,
28 wakaleta magodoro na mabulangeti, mabakuri na vyungu, na ngano, unga wa
shayiri, nafaka zilizokaangwa, maharage, dengu, 29 asali, siagi, kondoo na samli, ili
kwamba Daudi na watu waliokuwa pamoja naye waweze kula. Kwani walisema,
“Watu wana njaa, wamechoka na wana kiu huko nyikani.”

# 18

1 Daudi akawahesabu askari waliokuwa pamoja naye na akaweka akida wa elfu
na akida wa mia juu yao. 2 Kisha Daudi akalipeleka jeshi, thelusi moja chini
ya Yoabu, thelusi nyingine chini ya Abishai mwana wa Seruya, ndugu wa Yoabu,
na thelusi nyingine tena chini ya Itai Mgiti. Mfalme akaliambia jeshi, “kwa
hakika mimi mwenyewe pia nitakwenda pamoja nanyi. 3 Lakini watu wakasema,
“Wewe usiende vitani, kwani ikiwa tutakimbia hawatatujari sisi, ama nusu yetu
wakifa hawatajari. Lakini wewe ni zaidi ya elfu kumi yetu sisi! Kwa hiyo ni
afadhari zaidi ukitusaidia ukiwa mjini.” 4 Hivyo mfalme akawajibu, “Nitafanya
lolote lionekanalo jema machoni penu.” Mfalme akasimama kati ya lango la mji
wakati jeshi lilipoondoka katika mamia na katika maelfu. 5 Mfalme akawaagiza
Yoabu, Abishai, na Itai kusema, “Mmtendee huyo kijana, Absalomu, kwa upole kwa
ajili yangu.” Watu wote wakasikia jinsi mfalme alivyowaagiza maakida kuhusu
Absalomu. 6 Hivyo jeshi likaenda nyikani dhidi ya Israeli; vita ikaenea katika msitu

wa Efraimu. 7 Jeshi la Israeli likashindwa mbele ya askari wa Daudi; kulikuwa
na machinjo makuu kwa watu elfu ishirini siku hiyo. 8 Vita ikaenea katika eneo
lote na watu wengi wakaangamizwa na msitu kuliko upanga. 9 Ikatukia kwamba
Absalomu akakutana na askari wa Daudi. Absalomu alikuwa amepanda juu ya
nyumbu wake na nyumbu akapita chini ya matawi manene ya mti wa mwaloni, na
kichwa chake kikanaswa katika matawi ya mti. Akaachwa akining'inia kati ya nchi
na anga wakati nyumbu alipoendelea mbele. 10 Mtu mmoja akaona lililotukia na
akamwambia Yoabu, "Tazama, nilimwona Absalomu akining'inia katika mwaloni!"
11 Yoabu akamwambia aliyemwambia kuhusu Absalomu, "Tazama! Ulimwona!
Kwa nini haukumpiga hata chini. Ningekupa shekeli kumi za fedha na mkanda."
12 Yule mtu akamjibu Yoabu, "Hata kama ningepewa shekeli elfu za fedha hata
hivyo nisingeinua mkono wangu juu ya mwana wa mfalme, kwa maana sisi sote
tulimsikia mfalme akiwaagiza wewe, Abishai na Itai kusema, mtu asimguse huyo
kijana Absalomu.' 13 Ikiwa ningehatarisha maisha yangu kwa uongo(na hakuna
jambo linalofichika kwa mfalme), ungejitenga nami." 14 Ndipo Yoabu aliposema,
"sitakusubiri." Kisha akachukua mishale mitatu mkononi mwake na akairusha katika
moyo wa Absalomu wakati yu ngali hai na amening'inia katika mwaloni. 15 Kisha
vijana kumi waliochukua slaha za Yoabu wakamzunguka Absalomu, wakampiga na
kumwua. 16 Kisha Yoabu akapiga tarumbeta na jeshi likarudi kutoka kuwafuatia
Israeli, hivyo Yoabu akalirudisha jeshi. 17 Wakamchukua Absalomu na kumtupa
katika shimo kubwa msituni; wakaufukia mwili wake chini ya rundo kubwa la
mawe, wakati Israeli wote walipokimbia kila mtu nyumbani kwake. 18 Wakati
Absalomu alipokuwa yu ngali hai alijijengea nguzo kubwa ya jiwe katika Bonde
la Mfalme, kwani alisema, "Sina mwana wa kuchukua kumbukumbu ya jina
langu." Akaiita nguzo kwa jina lake, hivyo inaitwa Mnara wa Absalomu hata leo.
19 Kisha Ahimaasi mwana wa Sadoki akasema, "Niruhusu niende kwa mfalme na
habari njema, jinsi Yahwe alivyomwokoa kutoka mkono wa adui zake." 20 Yoabu
akamjibu, "Wewe hautakuwa mchukua habari leo; utafanya hivyo siku nyingine.
Leo hautachukua habari yoyote kwa maana mwana wa mfalme ameuawa." 21 Ndipo
Yoabu akamwambia Mkushi, "Nenda umwambia mfalme ulichokiona." Mkushi
akamwinamia Yoabu, na kisha akakimbia. 22 Kisha tena, Ahimaasi mwana wa Sadoki
akamwambia Yoabu, "Pamoja na yote yanayoweza kutokea, tafadhari niruhusu nami
pia niende nimfuate Mkushi." Yoabu akajibu, "Mwanangu kwa nini unataka kwenda,
hautapata thawabu yoyote kwa ajili ya habari hii?" 23 "Vyovyote itakavyokuwa
niache niende," Ahimaasi alijibu. Hivyo Yoabu akamjibu, "Nenda." Ndipo Ahimaasi
akakimbia kwa njia ya tambarare na akampita Mkushi. 24 Basi Daudi alikuwa amekaa
kati ya lango la ndani na lango la nje. Na mlinzi alikuwa juu ya lango ukutani
naye akainua macho yake. Alipokuwa akiangalia, akamwona mtu anakaribia huku
akikimbia peke yake. 25 Mlinzi akaita kwa sauti na kumwambia mfalme. Ndipo
mfalme akasema, "Ikiwa yupo peke yake ana habari katika kinywa chake." Mkimbiaji
akasogea na kuukaribia mji. 26 Kisha mlinzi akaona mtu mwingine aliyekuwa
anakimbia, naye akamwambia bawabu; kusema, "Tazama, kuna mtu mwingine
anakimbia peke yake." Mfalme akasema, "Yeye pia analeta habari." 27 Ndipo
mlinzi akasema, Nadhani kukimbia kwake mtu aliye mbele ni kama kukimbia kwake
Ahimaasi mwana wa Sadoki." Mfalme akasema, "Yeye ni mtu mwema naye anakuja
na habari njema." 28 Ndipo Ahimaasi akaita na kumwambia mfalme, "Yote ni
mema." Kisha akainama yeye mwenyewe uso wake chini mbele ya mfalme na
kusema, Atukuzwe Yahwe Mungu wako, aliyewatoa watu walioinua mkono wao
kinyume cha bwana wangu mfalme." 29 Hivyo mfalme akauliza, "Je huyo kijana
Absalomu hajambo?" Ahimaasi akajibu, "Wakati Yoabu ananituma kwako mfalme,

mimi mtumishi wa mfalme, niliona fujo kubwa sana lakini sikutambua ilihusu nini."
30 Mfalme akamwambia, "Geuka usimame kando." Hivyo Ahimaasi akageuka na
kusimama. 31 Mara Mkushi akafika na kusema, "Kuna habari njema kwa bwana
wangu mfalme kwa kuwa leo Yahwe amekulipia kisasi kwa wale wote walioinuka
kinyume chako." 32 Ndipo mfalme akamwuliza, "Je huyo kijana Absalomu ni mzima?"
Mkushi akajibu, "Adui wa bwana wangu mfalme na wote wainukao kukudhuru na
wawe kama huyo kijana." 33 Ndipo mfalme alipohuzunishwa sana naye akaenda
chumbani juu ya lango na kulia. Kadili alivyokwenda aliomboleza, mwanangu
Absalomu, mwanangu, mwanangu Absalomu! afadhari ningekufa badala yako,
Absalomu, mwanangu, mwanangu!"

# 19

1 Yoabu akaambiwa, "Tazama, mfalme analia na kumwombolea Absalomu."
2 Hivyo siku ile ushindi uligeuzwa kuwa maombolezo kwa jeshi lote, kwa maana jeshi
likasikia ikisemwa siku hiyo, "Mfalme anaomboleza kwa ajili ya mwanaye." 3 Siku ile
askari waliingia mjini kwa kunyemelea kimyakimya kama watu waonao haya baada
ya kukimbia vitani. 4 Mfalme akafunika uso wake na kulia kwa sauti, "Mwanangu
Absalomu, Absalomu, mwanangu, mwangangu!" 5 Ndipo Yoabu akaingia ndani kwa
mfalme na kumwambia, "Leo umeziaibisha nyuso za askari wako, waliookoa maisha
yako leo, maisha ya wanao na binti zako, maisha ya wake zako na maisha ya masuria
wako, 6 kwa maana wawapenda wakuchukiao na kuwachukia wakupendao. Kwa
kuwa leo umeonesha kwamba maakida na askari si chochote kwako. Natambua
sasa kwamba kame Absalomu angesalia na sisi sote tungekufa hilo lingekufurahisha.
7 Sasa basi, inuka na uende kuongea na askari wako kwa upole, kwani nakuapia
kwa Yahwe, ikiwa hutakwenda hakuna mtu hata mmoja atakayesalia nawe usiku
huu. Na hii itakuwa vibaya sana kwako kuliko madhara yoyote yaliyowai kukupata
tangu ujana wako." 8 Hivyo mfalme akainuka na kuketi kati ya lango la mji, watu
wote wakaambiwa, "Tazama, mfalme ameketi kati ya lango." Ndipo watu wote
wakaja mbele za mfalme. Walakini, Israeli walikimbia kila mtu nyumbani kwake.
9 Watu wote wakahojiana wao kwa wao katika jamaa zote za Israeli kusema, "Mfalme
alituokoa na mkono wa adui zetu. Alitukomboa na mkono wa Wafilisti lakini
sasa ameikimbia nchi mbele ya Absalomu. 10 Na Absalomu tuliyemtia mafuta juu
yetu amekufa vitani. Hivyo kwa nini hatuongei juu ya kumrudisha mfalme tena?"
11 Mfalme Daudi akatuma kwa Sadoki na kwa Abiathari makuhani kusema, "Ongeeni
na wazee wa Yuda kusema, Kwa nini ninyi mmekuwa wa mwisho kumrudisha
mfalme kwenye kasri lake tena, kwa vile usemi wa Israeli wote unamtaka mfalme
arudi katika kasri lake? 12 Ninyi ni ndugu zangu, mwili na mifupa yangu. Kwa nini
basi mmekuwa wa mwisho kumrudisha mfalme?' 13 Na mwambieni Amasa, 'Je wewe
si mwili na mfupa wangu? Mungu anifanyie hivyo na kuzidi pia ikiwa hautakuwa
jamadari wa jeshi langu tangu sasa na baadaye mahali pa Yoabu. 14 Naye akaishinda
mioyo ya watu wote wa Yuda kama mtu mmoja, hata wakatuma kwa mfalme kusema,
"Rudi sasa na watu wako wote." 15 Hivyo mfalme akarudi naye akaja Yordani. Na
watu wa Yuda wakaja Gilgali kwenda kumlaki mfalme ili kumvusha mfalme juu ya
Yordani. 16 Shimei mwana wa Gera, Mbenjamini, kutoka Bahurimu, akaharakisha
kushuka pamoja na watu wa Yuda ili kumlaki mfalme Daudi. 17 Kulikuwa na watu
elfu moja kutoka Benjamini waliokuwa pamoja naye, na Siba mtumishi wa Sauli
na wanawe kumi na watano na watumish wake ishirini walikuwa pamoja naye.
Wakavuka Yordani mbele za mfalme. 18 Wakavuka ili kuivusha familia ya mfalme
na kumfanyia lolote aliloona jema. Shimei mwana wa Gera akainama chini mbele za
mfalme mara alipoanza kuuvuka Yordani. 19 Shimei akamwambia mfalme, "Bwana

wangu asinione mwenye hatia au kuyaweka moyoni ambayo mtumishi wake alifanya
kwa ukaidi siku bwana wangu mfalme alipoondoka Yerusalemu. Tafadhari, mfalme
na asiyaweke moyoni. [20] Kwa maana mtumishi wako anatambua kwamba amekosa.
Tazama, ndiyo maana nimekuja leo wa kwanza katika nyumba ya Yusufu ili kumlaki
bwana wangu mfalme." [21] Lakini Abishai mwana wa Seruya akajibu na kusema, "Je
Shimei asife kwa hili kwa vile alivyomlaani mtiwa mafuta wa Yahweh?" [22] Ndipo
Daudi akasema, "Nifanye nini nanyi enyi wana wa Seruya, hata leo mkawa adui
zangu? Je mtu yeyote atauawa leo katika Israeli? Kwani sijui kama leo mimi ni
mfalme juu ya Israeli? [23] Hivyo mfalme akamwambia Shimei, "Hautakufa." Mfalme
akamwahidi kwa kiapo. [24] Kisha Mefiboshethi mwana wa Sauli akashuka ili kumlaki
mfalme. Hakuwa ameivalisha miguu yake wala kunyoa ndevu zake wala kufua nguo
zake tangu siku mfalme alipoondoka hata siku aliporudi kwa amani. [25] Na hivyo
alipotoka Yerusalemu ili kumlaki mfalme, mfalme akamwambia, "Mefiboshethi Kwa
nini haukwenda pamoja nami?" [26] Akajibu, "Bwana wangu mfalme mtumishi wangu
alinidanganya, kwani nilisema, nitapanda juu ya punda ili niende na mfalme, kwa
kuwa mtumishi wako ni mlemavu.' [27] Mtumishi wangu Siba amenisemea uongo,
mtumishi wako, kwa bwana wangu mfalme. Lakini bwana wangu mfalme ni kama
malaika wa Mungu. Kwa hiyo fanya lililojema machoni pako. [28] Kwa maana
nyumba yote ya baba yangu walikuwa maiti mbele ya bwana wangu mfalme, lakini
ukamweka mtumishi wako miongoni mwao walao mezani pako. Kwa hiyo nililiye
haki gani zaidi kwa mfalme?" [29] "Kisha mfalme akamwambia, "Kwa nini kueleza yote
zaidi? Nimekwisha amua kwamba wewe na Siba mtagawana mashamba." [30] Ndipo
Mefiboshethi akamjibu mfalme, "Sawa, acha achukue yote kwa vile bwana wangu
mfalme amerudi salama nyumbani kwake." [31] Kisha Berzilai Mgileadi akashuka
kutoka Rogelimu ili avuke Yordani pamoja na mfalme, naye akamsaidia mfalme
kuuvuka Yordani. [32] Basi Berzilai alikuwa mzee sana mwenye umri wa miaka
themanini. Alikuwa amemsaidia mfalme kwa mahitaji alipokuwako Mahanaimu
kwani alikuwa na mali nyingi. [33] Mfalme akamwambia Berzilai, njoo pamoja nami,
nami nitaandaa kwa ajili yako huko Yerusalemu." [34] Berzilai akamjibu mfalme,
"Kwani kuna siku ngapi zilizosalia maishani mwangu, hata niende na mfalme huko
Yerusalemu? [35] Nina umri wa miaka themanini. Je naweza kutofautisha mema na
mabaya? Je mtumishi wako anaweza kuonja ninachokula au kunywa? Je naweza
kusikia sauti zaidi za wanaume na wanawake waimbao? Kwa nini basi mtumishi
wako awe mzigo kwa bwana wangu mfalme? [36] Mtumishi wako angependa tu kuvuka
Yordani pamoja na mfalme. Kwa nini mfalme anilipe kwa thawabu kama hiyo?
[37] Tafadhari mruhusu mtumishi wako arudi nyumbani, ili kwamba nife katika mji
wangu katika kaburi la baba na mama yangu. Lakini tazama, huyu hapa mtumishi
wako Kimhamu. Haya yeye na avuke na bwana wangu mfalme na umfanyie lolote
lipendezalo kwako." [38] Mfalme akajibu, "Kimhamu atakwenda pamoja nami, nami
nitamtendea kila lionekanalo jema kwako, na lolote unalotamani kutoka kwangu
nitakutendea." [39] Kisha watu wote wakavuka Yordani, mfalme naye akavuka, kisha
mfalme akambusu Berzilai na kumbariki. Kisha Berzilai akarudi nyumbani kwake.
[40] Hivyo mfalme akavuka kuelekea Gilgali, na Kimhamu akavuka pamoja naye. Jeshi
la Yuda lote na nusu ya jeshi la Israeli likamleta mfalme. [41] Mara watu wa Israeli
wote wakaanza kuja kwa mfalme na kumwambia, "Kwa nini ndugu zetu, watu wa
Yuda, wamemwiba na kumleta mfalme na familia yake juu ya Yordani na watu wote
wa Daudi pamoja naye? [42] Hivyo watu wa Yuda wakawajibu watu wa Israeli, "Ni kwa
kuwa mfalme anahusiana nasi kwa karibu zaidi. Kwa nini basi mkasirike juu ya hili?
Je sisi tumekula chochote ambacho mfalme amekitoa? Je ametupa zawadi yoyote?
[43] Watu wa Israeli wakawajibu watu wa Yuda, Sisi tuna kabila kumi zaidi kwa mfalme

hivyo tuna sehemu kubwa zaidi kwa Daudi kuliko ninyi. Kwa nini basi mlitudharau? Je hatukuwa wa kwanza kupendekeza kumrudisha mfalme wetu? Lakini maneno ya watu wa Yuda hata yakawa makali kuliko maneno ya watu wa Israeli.

# 20

1 Ikatukia pia kuwa katika eneo lilelile kulikuwa mfanya fujo jina lake Sheba
mwana wa Bikri Mbenjamini. Akapiga tarumbeta na kusema, “Sisi hatuna sehemu
katika Daudi, wala hatuna urithi katika mwana wa Yese. Haya kila mtu na aende
nyumbani kwake, Israeli.” 2 Hivyo watu wote wa Israeli wakamwacha Daudi na
kumfuata Sheba mwana wa Bikri. Lakini watu wa Yuda wakamfuata mfalme wao
kwa karibu sana, kutoka Yordani njia yote hadi Yerusalemu. 3 Daudi alipofika katika
kasri lake huko Yerusalemu, akawachukua masuria aliokuwa amewaacha kulitunza
kasri, na akawaweka katika nyumba chini ya uangalizi. Aliwaandalia mahitaji yao
lakini hakulala nao tena. Hivyo walikuwa wametengwa hadi siku ya kufa kwao,
waliishi kama wajane. 4 Kisha mfalme akamwambia Amasa, “Uwaite watu wa
Yuda ndani ya siku hizi tatu; wewe pia uwepo hapa.” 5 Hivyo Amasa akaenda
kuwaalika watu wote wa Yuda kwa pamoja, lakini akatumia muda mrefu kulika
mfalme alivyokuwa amemwamuru. 6 Hivyo Daudi akamwambia Abishai, “Sasa Sheba
mwana wa Bikri atatufanyia madhara zaidi ya Absalomu. Chukua watumishi wa
bwana wako, askari wangu, na umfuatie asije akaingia katika mji wenye ngome
na kututoroka.” 7 Ndipo watu wa Yoabu wakamfuatia, pamoja na Wakerethi na
Wapelethi na mashujaa wote. Wakatoka Yerusalemu ili kumfuatia Sheba mwana
wa Bikri. 8 Walipokuwa katika jiwe kubwa lililoko Gibeoni, Amasa akaja kuwalaki.
Yoabu alikuwa amevaa silaha ya vita aliyokuwa ameivaa, alikuwa pia na upanga
uliokuwa umefungwa na mkanda katika kiuno chake. Kadili alivyoendelea mbele
upanga ukadondoka. 9 Hivyo Yoabu akamwambia Amasa, “Haujambo binamu
yangu?” Kwa utaratibu Yoabu akakishika kidevu cha Amasa kwa mkono wake
wa kulia ili ambusu. 10 Amasa hakutambua kwamba kulikuwa na jambia katika
mkono wa kushoto wa Yoabu. Yoabu akamchoma Amasa tumboni na matumbo yake
yakadondoka chini. Wala Yoabu hakumpiga tena, na Amasa akafa. Hivyo Yoabu
na Abishai nduguye wakamfuatia Sheba mwana wa Bikri. 11 Kisha mmoja wa watu
wa Yoabu akasimama kando ya Amasa naye akasema, “Aliye upande wa Yoabu na
aliyeupande wa Daudi na amfuate Yoabu.” 12 Amasa akawa anagalagala katika damu
yake katikati ya njia. Mtu yule alipoona kwamba watu wote wamesimama, akambeba
Amasa na kumweka shambani kando ya njia. Akatupa vazi juu yake kwa maana
aliona kila mmoja aliyekuja alisimamaa pale. 13 Baada ya Amasa kuondolewa njiani
watu wote wakamfuata Yoabu katika kumfuatia Sheba mwana wa Bikri. 14 Sheba
akazipita kabila zote za Israeli mpaka Abeli wa Beth Maaka, na katika nchi yote ya
Berite ambao pia walijikusanya pamoja pia na kumfuatia Sheba. 15 Walimpata na
kumzingira huko Abeli wa Bethi Maaka. Wakajenga buruji ya kuhusuru mji nyuma
ya ukuta. Jeshi lote lilokuwa pamoja na Yoabu likaugongagonga ukuta ili uanguke.
16 Ndipo mwanamke mwerevu akapiga kelele kutoka ndani ya mji, “Sikiliza, Yoabu,
tafadhari sikiliza! Sogea karibu nami ili niongee nawe.” 17 Hivyo Yoabu akakaribia,
mwanamke akamwambia, “Je wewe ni Yoabu? Akajibu, “ni mimi.” mwanamke
akamwambia, “Sikiliza maneno ya mtumishi wako.” Akajibu, “Nasikiliza.” 18 Ndipo
aliposema,”Hapo zamani ilisemwa, 'Bila shaka tafuteni ushauri huko Abeli,' na
kwamba ushauri huo utakata maneno. 19 Sisi ni mji ulio miongoni mwa miji yenye
nguvu na aminifu sana katika Israeli. Mnataka kuharibu mji ambao ni mama katika
Israeli. Kwa nini unataka kuumeza urithi wa Yahwe?” 20 Ndipo Yoabu alipojibu
na kusema, “Iwe mbali, iwe mbali nami, hata nikameze au kuharibu. 21 Hiyo si

kweli. Lakini mtu kutoka katika nchi ya milima ya Efraimu, aitwaye Sheba mwana
wa Bikri, ameinua mkono wake kinyume cha mfalme, kinyume cha Daudi. Mtoeni
yeye nami nitauacha mji." Mwanamke akamwambia Yoabu, "Utarushiwa kichwa
chake kutoka juu ya ukuta." 22 Kisha mwanamke akawaendea watu wote wa mji kwa
hekima yake. Wakakiondoa kichwa cha Sheba mwana wa Bikri na kumrushia Yoabu.
Ndipo alipopiga tarumbeta na watu wa Yoabu wakauacha mji kila mtu nyumbani
kwake. Na Yoabu akarejea Yerusalemu kwa mfalme. 23 Yoabu alikuwa juu ya jeshi
lote la Israeli na Benaya mwana wa Yehoiada alikuwa juu ya Wakerethi na Wapelethi.
24 Adoramu alikuwa juu ya watu waliofanya kazi ya shokoa na Yehoshafati mwana wa
Ahiludi alikuwa mkumbushaji. 25 Sheva alikuwa mwandishi, na Sadoki na Abiathari
walikuwa makuhani. 26 Ira wa Yairi alikuwa mhudumu mkuu wa Daudi.

# 21

1 Kulikuwa na njaa kwa miaka mitatu katika siku za utawala wa Daudi, na
Daudi akautafuta uso wa Yahwe. "Hivyo Yahwe akasema, "njaa hii ni kwa sababu
ya mauaji ya Sauli na familia yake, kwa kuwa aliwauwa Wagibeoni." 2 Basi
Wagibeoni hawakuwa uzao wa Israeli; walikuwa ni masalia ya Waamori. Watu wa
Israeli walikuwa wameapa kutowauwa, lakini Sauli alitaka kuwaangamiza wote kwa
husuda kwa ajili ya watu wa Israeli na Yuda. 3 Ndipo Daudi alipowaita pamoja
Wagibeoni na kuwaambia, "Niwafanyie nini kwa ajili ya upatanisho? Ili kwamba
mweze kuwabariki watu wa Yahwe wanaorithi wema na ahadi zake?" 4 Wagibeoni
wakamjibu, "Hili siyo jambo la fedha wala dhahabu kati yatu na Sauli au familia
yake. Na siyo hitaji letu kumwua mtu yeyote katika Israeli." Daudi akasema,
"Chochote mtakacho omba nitawafanyia." 5 Wakamjibu mfalme, "Mtu aliyetaka
kutuuwa aliyepanga kunyume chetu, ili kutuangamiza na kukosa eneo katika mipaka
ya Israeli - 6 haya na tupewe watu saba kutoka katika uzao wake, nasi tutawatundika
mbele ya Yahwe katika Gibea ya Sauli, palipochaguliwa na Yahwe." Mfalme akasema,
"Nitawapeni" 7 Lakini mfalme akamwifadhi Mefiboshethi mwana wa Yonathani
mwana wa Sauli, kwa ajili ya kiapo cha Yahwe kati ya Daudi na Yonathani mwana wa
Sauli. 8 Mfalme akawachukua wana wawili wa Rispa binti Ayia aliomzalia Sauli, hawa
wana wawili waliitwa Armoni na Mefiboshethi; na pia Daudi akawachukua wana
watano wa Mikali binti Sauli, aliomzalia Adrieli mwana wa Berzilai Mmeholathi.
9 Akawaweka katika mikono ya Wagibeoni. Nao wakawatundika juu ya mlima mbele
za Bwana, na wote saba wakafa pamoja. Waliuawa katika kipindi cha mavuno,
katika siku ya kwanza mwanzoni mwa mavuno ya shayiri. 10 Kisha Rispa, binti
Aiya, akachukua nguo ya gunia na akajitanda mwenyewe juu ya mlima kando
ya miili ya waliokufa tangu mwanzo wa mavuno mpaka wakati mvua ilipoanza
kunyesha. Hakuruhusu ndege wa angani kutua juu ya miili mchana wala ayawani
wa mwituni wakati wa usiku. 11 Daudi akaambia alichokifanya Rispa, binti Aiya,
suria wa Sauli. 12 Hivyo Daudi akaenda na kuchukua mifupa ya Sauli na mifupa
ya Yonathani mwanawe kutoka kwa watu wa Yabeshi Gileadi, waliokuwa wameiiba
kutoka katika eneo la jumuiya la Beth Shani, Wafilisti walipokuwa wamewatundika
baada ya Wafilisti kumwua Sauli katika Gilboa. 13 Daudi akaiondoa pale mifupa
ya Sauli na mifupa ya Yonathani mwanawe, na wakakusanya pia mifupa ya wale
watu saba waliotundikwa. 14 Wakaizika mifupa ya Sauli na Yonathani mwanawe
huko Zela katika nchi ya Benjamini, katika kaburi la Kishi babaye. Wakafanya kila
alichoagiza mfalme. Ndipo Mungu akajibu maombi yao kwa ajili ya nchi. 15 Kisha
Wafilisti wakaenda tena katika vita na Israeli. Hivyo Daudi na jeshi lake wakashuka
na kupigana na Wafilisti. Akiwa vitani Daudi akachoshwa na vita. 16 Ishbibenobu,
wa uzao wa majitu, ambaye mkuki wake wa shaba ulikuwa na uzito wa shekeli mia

tatu na alikuwa na upanga mpya, alitaka kumwua Daudi. [17] Lakini Abishai mwana
wa Seruya akamwokoa Daudi, akampiga Mfilisti na kumwua. Ndipo watu wa Daudi
wakamwapia, kusema, “Hautakwenda vitani pamoja nasi tena usije ukaizima taa ya
Israeli.” [18] Ikawa baadaye kuwa na vita tena kati ya Wafilisti huko Gobu, wakati
Sibekai Mhushathi alipomwua Safu, aliyekuwa miongoni mwa uzao wa Warefai.
[19] Ikawa tena katika vita na Wafilisti huko Gobu, huyo Elhanani mwana wa Jari
Mbethlehemu akamwua Goliathi Mgiti, ambaye fumo la mkuki wake lilikuwa kama
mti wa mfumaji. [20] Ikawa katika vita nyingine huko Gathi kulikuwa na mtu mrefu
sana mwenye vidole sita katika kila mkono na vidole sita katika kila mguu, jumla
yake ishirini na vinne. Yeye naye alikuwa wa uzao wa Warefai. [21] Alipowatukana
Israeli, Yonathani mwana mwana wa Shama, nduguye Daudi, akamwua. [22] Hawa
walikuwa wa uzao wa Warefai wa Gathi, waliuawa kwa mkono wa Daudi na kwa
mkono wa askari wake

# 22

[1] Daudi akamwimbia Yahwe maneno ya wimbo huu siku ile Yahwe alipomwokoa
katika mkono wa adui zake wote na katika mkono wa Sauli. [2] Akaomba hivi,
“Yahwe ni mwamba wangu, ngome yangu, aliyeniokoa. [3] Mungu ni mwamba
wangu. Yeye ni kimbilio langu. Ngao yangu, pembe ya wokovu wangu, ngome
yangu na kimbilio langu, aniokoaye na mabaya yote. [4] Nitamwita Yahwe, astahiliye
kutukuzwa, nami nitaokolewa kutoka kwa adui zangu. [5] Maana mawimbi ya mauti
yalinizunguka, mafuriko ya maji ya uharibifu yakanishinda. [6] Vifungo vya kuzimu
vilinizunguka; kamba za mauti zikaninasa. [7] Katika shida yangu nalimwita Yahwe;
nilimwita Mungu wangu; akaisikia sauti yangu katika hekalu lake, na kilio changu
cha msaada kikafika masikioni mwake. [8] Ndipo nchi ilipotikisika na kutetemeka.
Misingi ya mbingu ikatetemeka na kutikiswa, kwa kuwa Mungu alikasirika. [9] Moshi
ukatoka katika pua yake, na miale ya moto ikatoka katika kinywa chake. Makaa
yakawashwa nayo. [10] Alizifungua mbingu akashuka, na giza totoro lilikuwa chini
ya miguu yake. [11] Alipanda juu ya kerubi na kuruka. Alionekana katika mawingu
ya upepo. [12] Naye akalifanya giza kuwa hema kumzunguka, akakusanya mawingu
makubwa ya mvua angani. [13] Makaa ya moto yalidondoka mbele zake kutoka katika
radi. [14] Yahwe alishuka kutoka katika mbingu. Aliyejuu alipiga kelele. [15] Alipiga
mishale na kuwatawanya adui zake—miale ya radi na kuwasambaratisha. [16] Kisha
njia za maji zikaonekana; misingi ya dunia ikawa wazi katika kilio cha vita ya
Yahweh, katika sauti za pumzi ya pua zake. [17] Kutoka juu alifika chini; akanishikilia!
Aliniondoa katika vilindi vya maji. [18] Aliniokoa kutoka kwa adui zangu wenye nguvu,
kwao walionichukia, kwa maana walikuwa na nguvu sana kwangu. [19] Walikuja
kinyume changu siku ya shida yangu, lakini Yahwe alikuwa msaada wangu. [20] Pia
aliniweka mahali panapo nafasi. Aliniokoa kwa kuwa alipendezwa nami. [21] Yahwe
amenituza kwa kipimo cha haki yangu; amenirejesha kwa kiwango cha usafi wa
mikono yangu. [22] Kwa maana nimezishika njia za Yahwe na sijafanya uovu kwa
kugeuka kutoka kwa Mungu. [23] Kwa kuwa maagizo yake yote ya haki yamekuwa
mbele yangu; kwa kuwa sheria zake, sikujiepusha nazo. [24] Nimekuwa bila hatia
mbele zake pia, na nimejiepusha na dhambi. [25] Kwa hiyo Yahwe amenirejesha
kwa kiasi cha uadilifu wangu, kwa kipimo cha usafi wangu mbele zake. [26] Kwa
mwaminifu, unajionesha kuwa mwaminifu; kwake asiye na hatia; unajionesha kuwa
hauna hatia. [27] Kwa usafi unajionesha kuwa msafi, lakini kwa wakaidi unajionesha
kuwa mkaidi. [28] Unaokoa walioteswa, lakini macho yako ni kinyume cha wenye
kiburi, unawashusha chini. [29] Kwa maana wewe ni taa yangu, Yahwe. Yahwe
huangaza katika giza langu. [30] Maana kwa ajili yake ninaweza kupita vipingamizi;

kwa msaada wa Mungu wangu naweza kuruka juu ya ukuta. 31 Maana njia za
Mungu ni kamilifu. Neno la Yahwe ni safi. Yeye ni ngao yao wanaomkimbilia.
32 Maana ni nani aliye Mungu isipokuwa Yahwe? Na ni nani aliyemwamba isipokuwa
Mungu? 33 Mungu ni kimbilio langu, na umwongoza katika njia yake mtu asiye
na hatia. 34 Huifanya myepesi miguu yangu kama kurungu na kuniweka katika
vilima virefu. 35 Huifundisha mikono yangu kwa vita, na viganja vyangu kupinda
upinde wa shaba. 36 Umenipa ngao ya wokovu wako, na matakwa yako yamenifanya
mkuu. 37 Umeitengenezea miguu yangu nafasi chini yangu, hivyo miguu yangu
haikujikwaa. 38 Niliwafuatia adui zangu na kuwaangamiza. Sikurudi nyuma
hadi walipoangamizwa. 39 Niliwararua na kuwasambaratisha; hawawezi kuinuka.
Wameanguka chini ya miguu yangu. 40 Unaweka nguvu ndani yangu kama mkanda
kwa vita; unawaweka chini yangu wanaoinuka kinyume changu. 41 Ulinipa migongo
ya shingo za adui zangu; niliwaangamiza kabisa wale wanaonichukia. 42 Walilia
kwa msaada, lakini hakuna aliyewaokoa; walimlilia Yahwe, lakini hakuwajibu.
43 Niliwaponda katika vipande kama mavumbi juu ya ardhi, niliwakanyaga kama
matope mitaani. 44 Umeniokoa pia kutoka katika mashutumu ya watu wangu.
Umeniweka kama kichwa cha mataifa. Watu nisiowajua wananitumikia. 45 Wageni
walishurutishwa kuniinamia. Mara waliposikia kuhusu mimi, walinitii. 46 Wageni
walikuja wakitetemeka kutoka katika ngome zao. 47 Yahwe anaishi! Mwamba wangu
atukuzwe. Mungu na ainuliwe, mwamba wa wokovu wangu. 48 Huyu ndiye Mungu
anilipiaye kisasi, awawekaye watu chini yangu. 49 Uniweka huru mbali na adui
zangu. Hakika, uliniinua juu yao walioinuka kinyume changu. Uliniokoa kutoka kwa
watu wenye ghasia. 50 Kwa hiyo nitakushukuru, Yahwe, kati ya mataifa; nitaliimbia
sifa jina lako. 51 Mungu hutoa ushindi mkuu kwa mfalme wake, na uonesha uaminifu
wake wa kiagano kwa mtiwa mafuta wake, kwa Daudi na uzao wake daima."

# 23

1 Haya ni maneno ya mwisho ya Daudi-Daudi mwana wa Yese, mtu aliyeheshimiwa
sana, aliyetiwa mafuta na Mungu wa Yakobo, mwandishi mzuri wa zaburi wa
Israeli. 2 "Roho ya Yahwe alisema nami, na neno lake lilikuwa ulimini mwangu.
3 Mungu wa Israeli alinena, Mwamba wa Israeli aliniambia, "Atawalaye kwa haki
juu yangu, atawalaye katika hofu ya Mungu. 4 Atakuwa kama nuru ya asubuhi
jua linapochomoza, asubuhi isiyo na mawingu, wakati mche mwororo unapochipua
kutoka ardhini kupitia mwangaza wa mng'ao wa jua baada ya mvua. 5 Hakika,
je familia yangu haiko hivi mbele za Mungu? Je hajafanya nami agano la milele,
taratibu la uhakika kwa kila njia? Je yeye haongezi wokovu wangu na kutimiza
kila hitaji langu? 6 Lakini yasiyofaa yote yatakuwa kama miiba na kutupwa mbali,
kwa maana haiwezekani kukusanywa kwa mikono. 7 Ayagusaye ni lazima atumie
chombo cha chuma au au fumo la mkuki. Ni lazima yachomwe mahali yalipo.
8 Haya ni majina ya askari wa Daudi: Yashobeamu Mhakmoni alikuwa kiongozi
wa mashujaa. Aliua watu mia nne wakati mmoja. 9 Baada yake alikuwa Elieza
mwana wa Dodo, mwana wa mwahohi, mmoja wa mashujaa watatu wa Daudi.
Alikuwepo walipowashinda Wafilisti waliokuwa wamekusanyika kwa vita, na wakati
watu wa Israeli walipokuwa wamekimbia. 10 Elieza akasimama na kuwapiga Wafilisti
mpaka mkono wake ukachoka, mpaka mkono wake ukang'ang'ania mpini wa upanga
wake. Siku hiyo Yahwe akatoa ushindi mkuu. Jeshi likarejea kwa ajili ya kuteka
tu nyara za waliouawa na Elieza. 11 Baada yake alikuwa Shama mwana wa Agee,
Mharari. Wafilisti wakajikusanya pamoja palipokuwa na shamba la dengu, na
jeshi likawakimbia. 12 Lakini Shama akasimama katikati ya shamba na kulitetea.
Aliwauwa Wafilisti, na Yahwe akaleta ushindi mkuu. 13 Watatu kati ya askari

thelathini walishuka kwa Daudi nyakati za mavuno, katika pango la Adulamu.
Jeshi la Wafilisti lilikuwa limepiga kambi katika bonde la Mrefai. 14 Wakati huo
Daudi alikuwa katika ngome yake, pangoni, wakati Wafilisti walikuwa wanaimilk
Bethlehemu. 15 Daudi alitamani maji na akasema, “Kama ingekuwa mtu mmoja
angenipa maji ya kunywa kutoka kisima kilichopo Bethlehemu, kisima kilichopo
langoni!” 16 Hivyo mashujaa hawa watatu wakapita kati ya jeshi la Wafilisti na
kuchota maji katika kisima cha Bethlehemu, kilichopo langoni. Wakachukua maji
na kuyaleta kwa Daudi, lakini yeye akakataa kuyanywa. Badala yake akayamwaga
mbele za Yahwe. 17 Kisha akasema, “Iwe mbali nami, Yahwe, kwamba niyanywe
haya. Je ninywe damu ya watu waliohatarisha maisha yao?” Hivyo akakataa
kuyanywa. Haya ni mambo yaliyofanywa na mashujaa watatu. 18 Abishai, nduguye
Yoabu na mwana wa Seruya, alikuwa akida wa watatu. Alipigana kwa mkuki
wake na watu mia tatu na akawauwa wote mara. Mara kwa mara alitajwa kati
ya mashujaa watatu. 19 Hakuwa maarufu kuliko wale watatu? Alifanywa akida
wao. Lakini, umaarufu wake haukulingana na umaarufu wa wale mashujaa watatu.
20 Benaya kutoka Kabseeli mwana wa Yehoyada; alikuwa mtu hodari aliyefanya
matendo makuu. Aliwauwa wana wawili wa Arieli wa Moabu. Pia alishuka shimoni
na kuuwa simba wakati wa theruji. 21 Na alimwua Mmisri aliyekuwa mtu mnene
sana. Mmisri alikuwa na mkuki mkononi, lakini Benaya alipigana naye kwa fimbo
tu. Aliuchukua mkuki mkononi mwa Mmisri na kisha kumwua nao. 22 Benaya
mwana wa Yehoyada alifanya matendo haya, naye alitajwa kati ya mashujaa watatu.
23 Alikuwa na heshima kuliko mashujaa thelathini kwa ujumla wao, lakini hakuwa
na heshima kama wale mashujaa watatu. Hata hivyo Daudi alimweka kuwa mlinzi
wake. 24 Wafuatao ni wale watu thelathini: Asaheli nduguye Yoabu, Elhanani mwana
wa Dodo kutoka Bethlehemu, 25 Shama Mharodi, Elika Mharodi, 26 Helesi Mpeloni, Ira
mwana wa Ikeshi Mtekoi, 27 Abi Ezeri Mwanathothi, Mebunai Mhushathi, 28 Salmoni
Mhahoi, Maharai Mnetofathi; 29 Helebu mwana wa Baana, Mnetofathi, Itai mwana
wa Rabai kutoka Gibea ya Wabenjamini, 30 Benaya Mpirathoni, Hidai wa mabonde ya
Gaashi. 31 Abieliboni Mwarbathi, Azmawethi Mbarhumi, 32 Eliaba Mshalboni, wana
wa Yasheni, Yonathani mwana wa Shama Mharari; 33 Ahiamu mwana wa Sharari
Mharari, 34 Elifeleti mwana wa Ahasbai Mmaakathi, Eliamu mwana wa Ahithofeli
Mgiloni, 35 Hezro Mkarmeli, Parai Mwarbi, 36 Igali mwana wa Nathani kutoka Soba,
Bani kutoka kabila la Gadi, 37 Zeleki Mwamoni, Naharai Mbeerothi, mbeba silaha wa
Yoabu mwana wa Seruya, 38 Ira Mwithri, Garebu Mwithri, 39 Uria Mhiti - jumla yao
thelathini na wanane.

# 24

1 Kisha hasira ya Yahwe ikawaka dhidi ya Israeli, naye akamchochea Daudi
kinyume chao kusema, “Nenda, ukawahesabu Israeli na Yuda.” 2 Mfalme
akamwambia Yoabu, jemedari wa jeshi, aliyekuwa pamoja naye, “Nenda upite katika
kabila zote za Israeli, toka Dani mpaka Beersheba, uwahesabu watu wote, ili niweze
kujua idadi kamili ya watu wanaofaa kwa vita.” 3 Yoabu akamwambia mfalme,
“Yahwe Mungu wako na aizidishe hesabu ya watu mara mia, na macho ya bwana
wangu mfalme yaone ikifanyika. Lakini kwa nini bwana wangu mfalme analitaka
jambo hili? 4 Walakini neno la mfalme lilikuwa la mwisho dhidi ya Yoabu na dhidhi
ya majemedari wa jeshi. Hivyo Yoabu na majemedari wakatoka mbele ya mfalme
kuwahesabu watu wa Israeli. 5 Wakavuka Yordani na kupiga kambi karibu na Aroeri,
kusini mwa mji bondeni. Kisha wakasafiri kupitia Gadi mpaka Yazeri. 6 Wakaja
Gileadi na nchi ya Tahtimu Hodshi, kisha Dani, Jaani na karibu kuelekea Sidoni.
7 Wakafika ngome ya Tiro na miji yote ya Wahivi na Wakanaani. Kisha wakaenda
Negebu katika Yuda huko Beersheba. 8 Walipokuwa wamepita katika nchi yote,

wakarejea Yerusalemu mwishoni mwa miezi tisa na siku ishirini. 9 Ndipo Yoabu
alipotoa taarifa ya hesabu kamili kwa mfalme kuhusu watu wawezao kupigana vita.
Katika Israeli kulikuwa na watu 800, 000 jasiri wawezao kutoa upanga, na wale wa
Yuda walikuwa watu 500, 000. 10 Ndipo moyo wa Daudi ukamchoma alipokuwa
amewahesabu watu. Hivyo akamwambia Yahwe, “Kwa kufanya hivi nimetenda
dhambi sana. Sasa, Yahwe, uiondoe hatia ya mtumishi wako, kwani nimetenda
kwa upumbavu.” 11 Daudi alipoinuka asubuhi, neno la Yahwe likamjia nabii Gadi,
mwonaji wa Daudi, kusema, 12 Nenda umwambie Daudi; 'Hivi ndivyo asemavyo
Yahwe: “Ninakupa mambo matatu. Uchague mojawapo.” 13 Hivyo Gadi akaenda
kwa Daudi na kumwambia, “Je miaka mitatu ya njaa ije katika nchi yako? au miezi
mitatu ukimbie kutoka kwa adui zako huku wakikufuatia? au kuwe na tauni ya
siku tatu katika nchi yako? Amua sasa jibu gani nimrudishie aliyenituma.” 14 Ndipo
Daudi alipomwambia Gadi, “Nipo katika shida kubwa. Haya na tuanguke katika
mikono ya Yahwe kuliko kuanguka katika mikono ya mwanadamu, kwani matendo
yake ya rehema ni makuu sana.” 15 Hivyo akatuma tauni juu ya Israeli kuanzia
asubuhi kwa muda ulioamriwa, na watu sabini na tano elfu kutoka Dani mpaka
Beersheba wakafa. 16 Malaika aliponyosha mkono wake kuelekea Yerusalemu ili
kuuharibu, Yahwe akabadili nia yake kuhusu madhara, na akamwambia malaika
aliyekuwa tiyari kuwaangamiza watu, “Yatosha! Rudisha mkono wako sasa.”
Wakati huo malaika wa Yahwe alikuwa amesimama katika kiwanja cha kupuria
cha Arauna Myebusi. 17 Daudi alipomwona malaika aliyekuwa amewapiga watu,
akamwambia Yahwe kusema, “Nimetenda dhambi, na nimetenda kwa upumbavu.
Lakini kondoo hawa, wamefanya nini? Tafadhari, mkono wako na uniadhibu mimi
na familia ya baba yangu!” 18 Kisha Gadi akaja siku hiyo kwa Daudi na kumwambia,
“Kwea na ujenge madhabahu kwa ajili ya Yahwe katika kiwanja cha kupuria cha
Arauna Myebusi.” 19 Hivyo Daudi akakwea kama Gadi alivyomwelekeza kufanya,
kama Yahwe alivyokuwa ameagiza. 20 Arauna akatazama na kumwona mfalme na
watumishi wake wakikaribia. Ndipo Arauna akaondoka na kumsujudia mfalme uso
wake mpaka juu ya ardhi. 21 Kisha Arauna akasema, “Kwa nini bwana wangu
mfalme amekuja kwangu, mtumishi wake? Daudi akajibu, “Kununua uwanja wako
wa kupuria, ili nimjengee Yahwe madhabahu, ili kwamba tauni iondolewe kwa
watu.” 22 Arauna akamwambia Daudi, “Chukua liwe lako, bwana wangu mfalme.
Ulifanyie lolote lolote lililojema machoni pako. Tazama, ng'ombe kwa ajili ya sadaka
ya kuteketezwa na miganda ya kupuria na nira kwa kuni. 23 Haya yote bwana wangu
mfalme, mimi Arauna nakupa.” Kisha akamwambia mfalme, “Yahwe Mungu wako
na awe nawe.” 24 Mfalme akamwambia Arauna, “Hapana, nahimiza kukinunua
kwa thamani yake. Sitatoa kama sadaka ya kuteketezwa kwa Yahwe chochote
nisichokigharimia.” Hivyo Daudi akakinunua kiwanja cha kupuria na ng'ombe kwa
shekeli hamsini za fedha. 25 Daudi akajenga madhabahu kwa Yahwe pale na kutoa
juu yake sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani. Hivyo wakamsihi Yahwe kwa
niaba ya nchi, hivyo akaizuia tauni katika katika Israeli yote.

# 1Wafalme

1 Mfalme Daudi alipokuwa mzee sana, walimfunika kwa nguo, lakini hakupata
joto. 2 Kwa hiyo watumishi wake wakamwambia, “Na tutafute msichana bikra
kwa ajili ya mfalme bwana wetu. Ili amtumikie na kumtunza. Naye atalala
kwenye mikono yake ili bwana mfalme wetu apate joto. 3 Kwa hiyo wakatafuta
msichana mrembo katika mipaka yote ya Israeli. Wakampata Abishagi Mshunami
wakamlte kwa mfalme. 4 Yule msichana alikuwa mrembo sana. Naye akamtumikia
mfalme na kumtunza, Lakini mfalme hakumjua. 5 Wakati huo, Adoniya mwana wa
Hagithi alijiinua akisema, “Nitakuwa mfalme.” Kwa hiyo akajiandalia magari na
wapanda farasi hamsini ili wapige mbio mbele yake. 6 Baba yake alikuwa hajawahi
kumsumbua, kwa kusema, “kwa nini umefanya hili na lile?” Adoniya allikuwa
mwanamume mzuri sana aliyezaliwa baada ya Absalomu. 7 Akashauriana na Yoabu
mwana wa Seruya na Abiathari kuhani. Wakamfuata Adoniya wakamsaidia. 8 Lakini
Sadoki kuhani, Benaya mwana wa Yehoyada, nabii Nathani, Shimei, Rei, na watu
mashujaa wa Daudi hawakumfuata Adoniya. 9 Adoniya akataoa dhabihu za Kondoo,
na ndama walionona kwenye jiwe la Sohelethi, ambalo liko karibu na Eni Rogeli.
Akawakaribisha ndugu zake wote, watoto wa mfalme, wanaume wote wa Yuda, na
watumishi wa mfalme. 10 Lakini hakumkaribisha nabii Nathan, Benaya, wanaume
mashujaa, au ndugu yake Sulemani. 11 Kisha Nathani akamwambia Bethisheba
mama wa Sulemani, akaisema, “Je, haujasikia kuwa Adoniya mwana wa Hagathi
amekuwa mfalme, na Daudi bwana wetu halijui hilo? 12 Kwa hiyo sasa nakupa
ushauri, ili kwamba uweze kuokoa maisha yako na maisha ya mwanao Suleimani.
13 Nenda kwa mfalme Daudi; ukamwambie, 'Bwana wangu mfalme, Je, haukumwapia
mtumishi wako, ukisema, “Hakika Sulemani mwanao atatawala baada yangu, na
ataketi kwenye kiti changu cha enzi?” Kwa nini basi Adoniya anatawala?' 14 Wakati
ukiwa pale ukiongea na mfalme, Nitaingia baada yako na kuthibitisha hayo. 15 Kwa
hiyo Bathisheba akaingia chumbani kwa mfalme. Wakati huo mfalme alikuwa mzee
sana, na Abishagi Mshunami alikuwa akimtunza mfalme. 16 Bathisheba akaiinama
kifudifudi mbele ya mfalme. Na kisha mfalme akasema, “Una haja gani?” 17 Naye
akamwambia, “Bwana wangu, ulimwapia mtumishi wako kwa jina la BWANA, Mungu
wako, ukisema, 'Hakika Sulemani mwanao atatawala, baada yangu, naye ataketi
kwenye kiti changu cha enzi.' 18 Sasa, tazama, Adoniya ni mfalme, na bwana wangu
mfalme hajui jambo hili. 19 Ametoa dhabihu ya makisai, ndama walionona, na
kondoo wengi, na amewakaribisha wana wote wa mfalme, Abiathari kuhani, na
Yoabu jemedari wa jeshi, lakini hajamkaribisha Sulemani mtumishi wako. 20 Mfalme
bwana wangu, macho yote ya Israeli yako kwako, yakisubiri usemi wako juu ya nani
atakayeti kwenye kiti cha enzi baada yako, bwana wangu. 21 Vinginevyo itatokea,
wakati bwana wangu atakapolala na baba zake, kwamba Mimi na mwanangu
Sulemani kuhesabiwa wahaini.” 22 Wakati alipokuwa akiendelea na mfalme, nabii
Nathani aliingia. 23 Watumshi wakamwambia mfalme, “Nabii Nathani yuko hapa,”
Naye alipoingia mbele ya mfalme, akalala kifudifudi mbele ya mfalme na uso wake
ukielekea chini. 24 Nathani akamwambia, “Mfalme bwana wangu, Je, umesema,
Adoniya atatawala baada yangu, na ataketi kwenye kiti changu cha enzi? 25 kwani
leo ameshuka na ametoa dhabihu ya makisai, ndama walionona, na kondoo wengi,
na amewakaribisha wana wote wa mfalme, jemedari wa jeshi, na Abiatahari kuhani.
Nao wanakuka na kunywa mbele zake, na kusema, 'Mfalme Adoniya na aishi milele!'
26 Lakini mimi, mtumishi wako, Sadoki kuhani, Benaya mwana wa Yehoyada, na

mtumishi wako Suleimani, hajatukaribisha. 27 Je, bwana wangu mfalme amefanya
haya pasipo kutuambia sisi, watumishi wako, ni nani atakayeketi kwenye kiti cha
enzi baada yake?” 28 Ndipo mfalme Daudi lipojibu na kusema, “Mwiteni Bathisheba
arudi.” Naye akaja akasimama mbele ya mfalme. 29 Mfalme akafanya kiapo akasema,
“Kama BWANA aishivyo, ambaye ameniokoa toka tabu zote, 30 kama nilivyokuapia
kwa BWANA, Mungu wa Israeli, nikisema, 'Sulemani mwanao atatawala baada yangu,
naye ndiye atakayeketi kwenye kiti changu cha enzi, mahali pangu,' Nitafanya hivi
leo.” 31 Kisha Bathisheba akalala kifudifudi na sura yake ikielekea chini mbele ya
mfalme akasema, “Bwana wangu mfalme Daudi n a aishi milele!” 32 Mflme Daudi
akasema, “Niitieni Sadoki kuhani, nabii Nathani na Benaya mwana wa Yehoyada.”
Nao wakaja mbele ya mfalme. 33 Mfalme akawaambia, “Uwachukue watumishi
wangu, bwana wako, na umfanye Sulemani mwanangu apande juu ya nyumba yangu
mimi na mkamtelemshe mpaka chini Gihoni. 34 Na Sadoki kuhani na nabii Nathani
wamtawaze awe mfalme wa Israeli na tarumbeta zipigwe, 'Mfalme Suleimani na uishi
milele!' 35 Kisha njoni mkiwa nyuma yake, naye atakuja na kukaa kwenye kiti changu
cha enzi; kwani yeye ndiye atakayekuwa mfalme mahali pangu. Nimemchagua
yeye kuwa mtawala wa Israeli na Yuda.” 36 Benaya mwana wa Yehoyada akamjibu
mfalme, akasema, “Na iwe hivyo! Na BWANA, Mungu wa mfalme bwana wangu,
alithibitishe hilo. 37 Kama vile BWANA alivyokuwa na mfalme bwana wangu na
awe na Sulemani hivyo hivyo, na kuifanya enzi yake kuwa kubwa kuliko zaidi
ya enzi ya bwana wangu Daudi.” 38 Kwa hiyo Sadoki kuhani, nabii Nathani,
Benaya mwana wa Yehoyada, na Wakerethi na Wapelethi wakamfanya Sulemani
akapanda juu ya nyumba ya mfalme Daudi; wakamleta Gihoni. 39 Naye Sadoki kuhani
akachukua pembe lenye mafuta hemani akamtia mafuta Sulemani kisha wakapiga
tarumbeta, na watu wote wakasema, 'Mfalme Sulemani na aishi milele!' 40 Kisha
watu wote wakamfuata, na watu wakapiga zomari wakafurahi furaha kubwa mno,
kiasi kwamba dunia ikatetemeka kwa sauti zao. 41 Kisha Adoniya na wageni wake
waliokuwa pamoja naye wakasikia hayo walipomaliza kula. Yoabu alipozisikia sauti
za panda, akasema, “Kwa nini jiji lilko katika hali ya taharuki?” 42 Wakati alipokuwa
akiongea, Yonatahani mwana wa Abiathari kuhani alifika. Adoniya akamwambia,
“Karibu, 'kwa kuwa wewe wastahili kutuletea habari.” 43 Naye Yonathani akamjibu
Adoniya, “Mfalme bwana wetu Daudi amemfanya Sulemani kuwa mfalme. 44 Na
mfalme amemtuma pamoja naye Sadoki, nabii Nathani, Benaya mwana wa Yehoyada,
na Wakerethi pamoja na Wapelethi. Wamempandisha Sulemani juu ya nyumba
ya mfalme. 45 Sadoki kuhani na nabii Nathani wamemtawaza kuwa mfalme kule
Gihoni, na wametokea huko wakifurahi, ndiyo maana jiji liko katika taharuki. Na
hizi ndizo sauti ulizosikia. 46 Pia, Sulemani ameketi kwenye kiti cha enzi cha
ufalme. 47 Zaidi ya yote, watumishi wa mfalme walikuja kumbariki mfalme bwana
wetu Daudi, wakisema, 'Mungu wako na alifanye jina la Sulemani kuwa zuri kuliko
jina lako, na kuifanya enzi yako kuwa kubwa kuliko yako.' na mfalme akasujudu
mwenyewe kitandani. 48 Mfalme pia alisema, 'Abarikiwe BWANA, Mungu wa Israeli,
ambaye amempa mtu kuketi kwenye enzi yangu siku hii ya leo, na kwamba macho
yangu yamejionea hilo.'” 49 Ndipo wageni wote wa Adoniya walipoogopa sana.
Wakasimama na kila mtu akaenda njia yake. 50 Pia Adoniya alimwaogopa Sulemani
na akasimama, na akaondoka, akachukua pembe la madhabahuni. 51 Kisha Sulemani
akaambiwa hilo, wakasema, “Tazama, Adoniya amemwogopa mfalme Sulemani, kwa
kuwa ameshikilia pembe la madhabahuni, akisema, 'Mfalme Sulemani na aniapie
kwanza kuwa hatamwua mtumishi wake kwa upanga.'” 52 Sulemani akasema, “Kama
atajionyesha kuwa ni mtu wa kweli, hakuna hata unywele mmoja utakaoanguka
duniani, bali kama uovu utaonekana kwake, atakufa.” 53 Kwa hiyo mfalme Sulemani

akatuma watu, waliomleta Adoniya kutoka madhabahuni. Naye akaja akapiga magoti kwa Sulemani, na Sulemani akamwambia, “Nenda nyumbani kwako.”

# 2

1 Daudi alipokaribia kufa, alimwamuru Sulemani mwanae, akisema, 2 “Mimi sasa
ninaiendea njia ya dunia yote. Kwa hiyo, uwe imara, na ujionyeshe mwenyewe
kama mwanamume. Uzilinde amri za BWANA, Mungu wako ukitembea katika njia
zake, utii maaagizo yake, amari zake, 3 maamuzi yake, na maagizo ya maagano yake,
uwe mwamngalifu kufanya yale yaliyoandikwa katika sheria za Musa, ili ufanikiwe
katika yote utakayoyafanya, popote kule utakakokuwa, 4 na BWANA atayatimiza
maneno yake aliyosema kuhusu mimi, aliposema, 'kama wanao watajilinda katika
tabia zao, wakatembea mbele yangu kwa uaminifu kwa mioyo yao yote na kwa
roho zao zote, hawatakoma kuwa na mtu aliyeketi katika kiti cha enzi cha Israeli.
5 Wewe pia wajua kile Yoabu mwana wa Seruya alichonifanyia, na kile alichowafnyia
majemedari wa majeshi y a Israeli, kwa Abina mwana wa Neri, na kwa Amasa
mwana wa Yetheri, ambaye alimwua. Alimwaga damu vitani wakati wa amani na
kuiweka ile damu kwenye mshipi uliokuwa kiunoni mwake na kwenye vile viatu
miguuni mwake. 6 Mshughulikie Yoabu kwa hekima ambayo umejifunza, lakini
usiache mvi zake ziingie kaburini kwa amani. 7 Hata hivyo, uonyeshe utu kwa wana
wa Barizilai Mgileadi, na uwaache wawe miongoni mwa wale wanaokula mezani
kwako, kwa kuwa walikuja kwangu wakati nilipomkimbia ndugu yangu Absalomu.
8 Tazama, Shimei mwana wa Gera yuko pamoja na wewe, Wabenjamini wa Bahurimu,
walionilaani kwa laana ya fujo siku niliyoenda kwa Mahanaimu. Shimei alishuka
kuja kuniona pale Yorodani, na nikamwapia kwa BWANA, nikisema, 'Sitawaua kwa
upanga,' 9 Kwa hiyo sasa usimwache aiepuke adhabu. Wewe ni mwenye hekima,
na utajua jinsi itakavyokupasa kumtendea. Utakileta hicho kichwa chenye mvi chini
kaburini.” 10 Ndipo Daudi alipolala na mababu zake na alizikwa kwenye mji wa
Daudi. 11 Siku ambazo Daudi alitwala Israeli zilikuwani miaka arobaini. Alikuwa
ametawala kwa miaka saba kule Hebroni na kwa miaka thelethini na tatu kule
Yerusalemu. 12 Kisha Sulemani akaketi kwenye kiti cha enzi cha baba yake Daudi,
na utawala wake ulikuwa imara. 13 Kisha Adoniya mwana wa Hagathi alikuja kwa
Bathisheba mama wa Sulemani., Naye akamwuliza, “Je, unakuja kwa amani?” Naye
akajiibu. “kwa amani.” 14 Kisha akasema, “Nina jambo la kukuambia.” Naye akajibu,
“Sema.” 15 Adoniya amesema, “Unajua kuwa ufalme ulikuwa wangu, na kwamba Is-
raeli yote ilikuwa inanitegemea mimi kuwa mfalme. Hata hivyo, ufalme umegeuzwa
na umekuwa wa ndugu yangu, kwani ulikuwa wake toka kwa BWANA. 16 Sasa
nina ombi moja kwako. Usinikatalie.”Bathisheba akamwambia, “Sema.” 17 Naye
akamwambia, “Tafadhali mwambie mfalme Sulemani, kwa kuwa hatakukatalia, ili
kwamba anipatie Abishagi Mshunami awe mke wangu.” 18 Bathisheba akamwambia,
“Vyema sana, nitamwambia mfalme” 19 Kwa hiyo Bathisheba akaenda kumwambia,
mfalme Sulemani kwa niaba ya Adoniya. Mfalme akainuka kumlaki na akapiga
magoti mbele yake. Kisha akaa kwenye kiti chake cha enzi na kulikuwa na kiti
kingine cha enzi kilicholetwa kwa ajili ya mama wa mfalme. Naye akaa mkono
wa kuume wa mfalme. 20 Ndipo alipomwambia, “Napenda kukuomba ombi moja
dogo. Usinikalie.” Mfalme, akamjibu, “Mama omba kwa kuwa sitakukatalia.” 21 Naya
akamwambia, “Naomba Abishagi Mshunami apewe Adoniya ndugu yako awe mke
wake.” 22 Mfalme Sulemani akamjibu mama yake, “Kwa nini unamwombea Adoniya
huyo Abishagi Mshunami? Kwa nini usimwombee ufalme pia, kwa kuwa ni ndugu
yangu mkubwa? - au kwa Abiathari kuhani, au Yoabu mwana wa Seruya?” 23 Kisha
mfalme Sulemani akaapa kwa BWANA, akisema, “Mungu wangu na anifanyie hivyo,

na zaidi pia, kama Adoniya hajayasema haya kinyume na maisha yake. 24 Sasa
basi kama BWANA aishivyo, ambaye ndiye alinifanya mimi kuwepo na kunipa kiti
cha enzi cha Daudi baba yangu, na ambaye amenifanyia nyumba kwa ahadi yake,
hakika Adoniya lazima auawe leo." 25 Kwa hiyo mfalme Sulemani akamtuma Benaya
mwana wa Yehoyada naye akamkuta Adoniya na kumwua. 26 Kisha akamwambia
Abiathari kuhani, "Nenda kwa Anathothi, kwenye mashamba yako. unastahili kufa,
lakini sitakua sasa hivi, kwa sababu ulilbeba sanduku la BWANA mbele ya Daudi
baba yangu na kujitabisha kwa namna mbalimbali kama baba yangu alivyopata
tabu." 27 Kwa hiyo Sulemani akamfukuza Abiathari asiwe kuhani wa BWANA, ili
kwamba atimilize maneno ya BWANA, aliyokuwa amesema juu ya nyumba ya Eli.
28 Habari hizo zikamfikia Yoabu, Kwani Yoabu alimuunga mkono Adoniya, ingawa
hakumuunga mkono Absalomu. Kwa hiyo Yoabu akakimbilia kwenye hema ya
BWANA karibu na madhabahu na akabeba pembe za madhabahu. 29 Sulemani
alipoambiwa kuwa Yoabu amekimbilia kwenye hema ya BWANA na sasa alikuwa
karibu na madhabahu. Ndipo Sulemani alipomtuma Benaya mwana wa Yehoyada,
akisema, "Nenda, ukamwue." 30 Kwa hiyo Benaya akaenda kwenye hema ya BWANA
na kumwambia, "Mfalme anasema utoke hemani." Yoabu akamjibu, "Hapana, Nitafia
hapa," Kwa hiyo Benaya akarudi kwa mfalme, akasema, "Yoabu amesema atafia
kwenye madhabahu," 31 Naye mfalme akamwambia, "Kafanye kama alivyosema.
Muue na ukamzike, ili kwamba uitoe kwangu na kwenye nyumba ya baba yangu
damu ambayo Yoabu alimwaga bila sababu. 32 BWANA na amrudishie damu yake
kichwani kwake, kwa sababu aliwaua wanaume wawili wasio na hatia na wema
kuliko yeye na akawaua kwa upanga, Abineri mwana wa Neri, Jemedari wa Jeshi la
Israeli, na Amasa mwana wa Jetheri, jemedari wa jeshi la Yuda, bila baba yangu Daudi
kujua. 33 Kwa hiyo damu yao na imrudie Yoabu kichwani pake na kwenye vichwa vya
uzao wake milele na milele. Lakini kwa Daudi na uzao wake, na nyumba yake, na
kwenye kiti chake cha enzi, kuwe na amani ya kudumu kutoka kwa BWANA." 34 Kisha
Benaya mwana wa Yehoyada akaenda akamvamia Yoabu na kumwua. Alizikwa
kwenye nyumba yake kule jangwani. 35 Mfalme akamwinua Benaya mwana wa
Yehoyada kuwa juu ya jeshi badala yake, na akamweka Sadoki kuhani kwenye nafasi
ya Abiatahari. 36 Kisha Mfalme akatuma watu kumwita Shimei, na akamwambia,
"Kajijengee nyumba kwa ajili yako kule Yerusalemu na ushi huko, na usitoke nje ya
Huo mji na kwenda mahali pengine. 37 Kwa kuwa siku utakayoenda mahali pengine,
na kupita bonde la Kidroni, ujue kwa hakika kuwa utakufa. Damu yako itakuwa
juu ya kichwa chako." 38 Kwa hiyo Shimei akamwambia mfalme, "Unachosema ni
chema. Kama vike mfalme bwana wangu alivyosema, ndivyo ambavyo mtumishi
wako atakavyofanya." Kwa hiyo Shimei akaishi Yerusalemu kwa miaka mingi.
39 Lakiini mwishoni mwa mwaka wa tatu, watumishi wawili wa Shimei wakakimbilia
kwa Akishi mwana wa Maaka, mfalme wa Gathi. Kwa hiyo wakamwambia Shimei,
wakisema, "Tazama, watumishi wako wameenda Gathi," 40 Kisha Shimei akainuka,
akapanda punda wake akaenda kwa Akishi huko Gathi kuwatafuta watumishi wake.
Akaenda na akawaleta watumishi wake toka Gathi. 41 Sulemani alipoambiwa kuwa
Shimei alikuwa ametoka Yerusalemu kwenda Gathi na amerudi, 42 mfalme akatuma
wito kwa Shimei na kumwambia, "Je, sikukuapisha kwa BWANA na kushuhudia
kwako, nikisema, 'Tambua kuwa siku utakayotoka kwenda nje na kwenda mahali
popote, hakika utakufa'? Na ukaniambia kuwa unachosema ni chema.' 43 Kwa nini
basi umeshindwa kulinda kiapo chako kwa BWANA na amri niliyokupa?" 44 Pia
mfalme akamwambia Shimei, "Unajua katika moyo wako maovu yote uliyofanya
kwa baba yangu Daudi. Kwa hiyo BWANA atakurudishia maovu yako kichwani pako.
45 Lakini Sulemani atabarikiwa na enzi ya Daudi itaimarika mbele ya BWANA milele."

46 Kwa hiyo mfalme akamwamuru Benaya mwana wa Yehoyada kwenda kumwua Shimei. Kwa hiyo ule utawala ulikuwa mwema kwa mkono wa Sulemain.

# 3

1 Sulemani akawa na ushirikiano wa kindoa na Farao mfalme wa Misri. Alimwoa
binti wa Farao na kumleta katika mji wa Daudi mpaka alipomaliza kujenga nyumba
yake, nyumba ya BWANA, na ukuta wa Yerusalemu. 2 Watu walikuw wakitoa
sadaka kwenye maeneo ya juu, kwa sababu hapakuwa bado na nyumba iliyokuwa
imejengwa kwa jina la BWANA. 3 Sulemani alionyesha upendo wake kwa BWANA
kwa kutembea katika maagizo ya Daudi baba yake, isipokuwa tu alitoa dhabihu
na kuchoma uvumba mahali pa juu. 4 Mfalme akaenda Gibioni kutoa sadaka kule,
kwa kuwa hilo ndilo lilikuwa eneo kuu la juu. Sulemani katoa sadaka maelfu katika
madhabu hiyo. 5 BWANA akaonekana kwa Sulemani huko Gibioni katika ndoto ya
usiku; akasema, "Omba! uanataka nikupe nini?" 6 Kwa hiyo Sulemani akasema,
"umeonyesha uaminifu wa agano mkuu kwa mtumishi wako, Daudi baba yangu, kwa
sababu alitembea mbele yako kwa ukweli na uaminifu, katika haki ya moyo na katika
unyofu wa moyo. Umetunza kwa ajili yake hili agano kuu kwa uaminifu na umempa
mwana wake kuketi kwenye kiti chake cha enzi leo. 7 Na sasa, BWANA, Mungu
wangu, umemfanya mtumishi wako kuwa mfalme katika nafasi ya Daudi baba yangu,
japo mimi ni mtoto mdogo. Sijui namna ya kuiingia na kutoka. 8 Mtumishi wako
yuko katikati ya watu wako uliowachagua, kundi kubwa, watu wangi wasiohesabika.
9 Kwa hiyo umpe mtumishi wako moyo wa uelewa wa kuwahukumu watu wako.
Kwani ni nani awezaye kuwahukumu watu wako hawa walio wengi?" 10 Ombi
hili la Sulemani likampendeza Bwana. 11 Kwa hiyo Mungu akamwambia. "Kwa
sababu umeomba jambo hili na haujajiombea maisha marefu au utajiri au uhai wa
maadui wako, lakini umeomba ufahamu wa kutambua hukumu ya haki, 12 Tazama
sasa nitafanya yote uliyoniomba wakati uliponipa ombi lako. Ninakupa moyo wa
hekima na ufahamu, kwa kuwa hapajawahi kuwa na mtu wa kuwa kama wewe kabla
yako, na hakuna wa kuwa kama wewe atakayeinuka baada yako. 13 Pia ninakupa
hata ambayo hujaomba, vyote heshima na utajiri, ili kwamba pasije pakawa na
mfalme wa kuwa kama wewe katika siku zako zote. 14 Kama utatembea katika
njia zangu na kuyatunza maagizo yangu na maagizo yangu, kama alivyofanya baba
yako Daudi, ndipo nitakapoziongeza siku zako." 15 Kisha Sulemani alipoamka, na
tazama, ilikuwa ndoto. Akaja Yerusalemu na akasimama mbele ya sanduku na agano
la Bwana. Akatoa sadaka za kuteketezwa na sadaka za amani, na akawafanyia
sherehe watumishi wake wote. 16 Kisha wanawake wawili waliokuwa makahaba
wakaja mbele ya mfalme wakasimama mbele yake. 17 Mwanamke mmoja akasema,
"Aa, bwana wangu, mwanamke huyu na mimi tunaishi katika nyumba moja, Nilizaa
mtoto tukiwa pamoj na yeye katika nyumba yetu. 18 Ikatokea siku ya tatu baada ya
kujifungua na yeye akajifungua. Tulikuwa sisi tu. Hapakuwepo na mtu mwingine
yeyote katika nyumba yetu, ila sisi tu wawili katika hiyo nyumba. 19 Kisha mtoto wa
mwanamke huyu akafa wakati wa usiku, kwa sababu alimlalia. 20 kwa hiyo akamka
wakati huo wa usiku wa manane akamchukua mwanangu toka pembeni yangu,
wakati mimi mtumishi wako nilipokuwa usingizini, na akamlaza kwenye kifua chake,
na akamlaza mtoto wake aliyekufa juu ya kifua changu. 21 Asubuhi nilipoamka ili
kumhudumia mwanangu, nikaona kuwa alikuwa amekufa. Lakini nilipomwangalia
kwa makini wakati huo wa asubuhi, nikagundua kuwa hakuwa yule mwanangu
niliyezaa," 22 Yule mwanamke mwingine akasema, "Hapana, Huyu aliye hai ndiye
wangu. Na yule aliyekufa ndiye wako." Yule mwanamke wa kwanza akasema,
"Hapana, Yule mtoto aliyekufa ndiye mwanao, na huyu aliye hai ndiye wangu." Hivi

ndivyo walivyoongea mbele ya mfalme. 23 Kisha mfalme akasema, “Mmoja wenu
anasema, 'huyu aliye hai ni wangu, na kumbe mwanao ndiye aliye kufa,'na mwingine
naye anasema, 'Hapana, mwanao ni yule aliyekufa, na mwanangu ni huyu aliye hai.'”
24 Mfalme akasema, ''Nileteeni upanga.” Kwa hiyo wakaleta upanga kwa mfalme.
25 Kisha mfalme akasema, “Mgawe mtoto aliye hai katika vipande viwili, na huyu
mwanamke apewe nusu na yule mwingine naye apewe nusu.” 26 Yule mwanamke
mwenye mtoto aliyekuwa hai akamwambia mfalme, kwa kuwa moyo wake ulikuwa
na huruma sana kwa mwanae, akasema, “Aa, bwana wangu, mpatie huyu mtoto aliye
hai, na usimwue kamwe.” Lakini yule mwanamke mwingine akasema, “Hatakuwa
wangu wala wako. Mgawe.” 27 Ndipo mfalme aliposema, “Mpe yule mwanamke wa
kwanza mtoto aliye hai, na kamwe usimwue. Yeye ndiye mama wa mtoto huyu.”
28 Israeli wote waliposikia hukumu ambayo mafalme ametoa, walimwogopa mfalme,
kwa sababu waliona kuwa hekima ya Mungu ilikuwa ndani yake kwa ajili ya kutoa
kuhukumu.

# 4

1 Mfalme Sulemani alikuwa mfalme wa Israeli. 2 Hawa ndio waliokuwa wakuu
wake: Azaria mwana wa Sadoki alikuwa kuhani. 3 Elihorefu na Ahiya mwana wa
Shisha, walikuwa makatibu. Yehoshafati mwana wa Ahilui alikuwa mwandishi.
4 Benaya mwana wa Yehoyada alikuwa mkuu wa jeshi. Sadoki na Abiatahari
walikuwa makuhani. 5 Azaria mwana wa Natahani ndiye aliyekuwa juu ya hawa
maakida. Zabudi mwana wa Nathani alikuwa kuhani na rafiki wa mfalme. 6 Ahishari
alikuwa mkuu wa nyumba. Adoniramu mwana wa Abda alikuwa mkuu wa watenda
kazi. 7 Sulemani alikuwa na maakida kumi na wawili juu ya Israeli yote, ambao
walitoa chakula kwa mfalme na watu wake wote. Kila mtu alikuwa na zamu
ya kuhudumia kwa mwezi mmoja katka mwaka. 8 Majina yao yalikuwa ndiyo
haya: Beni Huri, Kutoka milima ya Efraimu; 9 Beni Dekeri wa Makazi, Shaalibimu,
Bethi Shemeshi, na Elonbethi Hanaan; 10 Beni Hesed, wa Arubothi (kutoka kwake
alipatikana Sokohi na nchi yote ya Hefa); 11 Ben Abinadabu, wa wilaya yote ya
Dori (alikuwa na Tafathi binti wa mfalme ambaye alikuwa mke wake); 12 Baana
mwana wa Ahiludi, wa Taanaki na Megido, na Beth Shani iliyo upande mwingine
wa Zarethani chini ya Yezreel, Kutoak Bethi Shani mpaka Abeli Mehola iliyo upande
mwingine wa Jokimeamu; 13 Ben Geberi, ya Ramothi Gileadi (kutoka kwake tunapata
miji ya Yairi mwana wa Manase, ambayo iko Gileadi, na mkoa wa Arigobu ulikuwa
wake, ambao uko Bashani, miji sitini yenye maboma na yenye nguzo za malango
ya shaba); 14 Ahinadabu mwana wa Ido, wa Mahanaimu; 15 Ahimaazi, wa Naftali
(ambaye pia alimwoa Basimathi binti wa Sulemani kuwa mke wake); 16 Baana mwana
wa Hushai, ya Asherina Bealothi; 17 Yehoshafati mwana wa Paruha, kwa Isakari;
18 Shimei mwana wa Ela, wa Benjamini; 19 na Geberi mwana wa Uri, katika nchi ya
Gileadi, ambayo ni nchi ya Sihoni mfalme wa Waamori na Ogi mfalme wa Bashani,
na yeye ndiye akida pekee aliyekuwa katika nchi hiyo. 20 Yuda na Israeli walikuwa
wengi kama mchanga wa baharini. Nao walikuwa wakila na kunywa na kufurahi.
21 Suleimani alitawala utawala wote kutoka mtoni hadi kwenye nchi ya Wafilisti na
hadi kwenye mpaka wa Misri. Wote walileta kodi na walimtumikia Sulemani katika
siku za maisha yake yote. 22 Mahitaji ya Sulemani kwa siku moja yalikuwa ni Kori
thelathini za unga mzuri na kori unga wa ngano, 23 makisai kumi walionona, na
fahari ishirini wa malisho, na kondoo mia moja, nje ya ayala, paa, na kulungu na
kuku walionona. 24 Kwa kuwa utawala wake ulikuwa zaidi ya nchi yote upande huu
wa mto, kutoka Tifsa mpaka Gaza, juu ya wafalme wote wa upande huu wa mto,
naye alikuwa na amani pande zote. 25 Yuda na Israeli waliishi kwa usalama, kila
mtu chini y a mzabibu wake na chini ya mtini wake, kutoka Dani mpaka Beerisheba,

siku zote za Sulemani. [26] Sulemani alikuwa na mabanda ya farasi arobaini elfu kwa ajili ya magari yake, na wapanda farasi elfu kumi na mbili. [27] Na maakida walileta chakula kwa Sulemani na kwa wale walioketi kwenye meza ya mfalme Sulemani, kila mtu katika mwezi wake. Walihakikisha hakuna kinachopungua. [28] Na pia walileta kwenye eneo husika shayiri na majani kwa ajili ya wale farasi wa magari na kwa wale farasi wa mbio kila mmoja alileta kadri alivyoweza. [29] Mungu alimpa Sulemani hekima kubwa, ufahamu, na upana wa uelewa kama mchanga wa baharini.
[30] Hekima ya Sulemani ilizidi hekima ya watu wote wa mashariki na hekima yote ya Misri. [31] Alikuwa na hekima kuliko wanaume wote - kuliko Ethani Muezrahi, Hemani, Kaliko, na Darda, wana wa Maholi - na habari zake zikaenea hadi kwenye mataifa yote yaliyomzunguka. [32] Aliongea mithali elfu tatu na idadi ya nyimbo zake zilikuwa elfu moja na tano. [33] Aliifafanua mimea, kuanzia mierezi iliyoko Lebanoni hadi Hisopo imeao ukutani. Aliwafafanua wanyama, ndege, vitu vitambaavyo na samaki. Watu walikuja kutoka mataifa yote kuisikia hekima ya Sulemani. [34] Watu walikuja kutoka falme zote za duniani waliosikia juu ya hekima yake.

# 5

[1] Hiramu mfalme wa Tiro aliwatuma watumishi wake kwa Sulemani kwa kuwa alisikia kuwa walikuwa wamemtawaza kuwa mfalme mahali pa baba yake, kwani Hiramu alimpenda Daudi. [2] Sulemani akatuma ujumbe kwa Hiramu, akisema,
[3] “Unajua kuwa Daudi baba yangu hakujenga nyumba kwa jina la BWANA, Mungu wake kwa sababu ya vile vita vilivyomzunguka, kwa kuwa wakati wa uhai wake BWANA alikuwa akiweka maadui wake chini ya nyayo za miguu yake. [4] Lakini sasa BWANA amenipa mimi pumziko toka pande zote. Hakuna maadui wala majanga.
[5] Kwa hiyo ninakusudia kujenga hekalu kwa jina la BWANA, Mungu wangu, kama BWANA alivyosema kwa Daudi baba yangu, akisema, 'Mwanao ambaye nitamweka kwenye kiti chako cha enzi mahali pako, ndiye atakayenijengea hekalu kwa jina langu.' [6] Kwa hiyo sasa amuru wakate mierezi kutoka Lebanoni kwa ajili yangu. Watumishi wangu wataungana na watumishi wako, nami nitakulipa kwa ajili ya watumishi wako ili kwamba upate malipo mazuri kwa kila kitu utakchokubali kukifanya. Kwa kuwa unajua kuwa hakuna mtu mioingoni mwetu anayejua kukata miti kama Wasidoni.” [7] Hiramu aliposikia maneno ya Sulemani, akafurahi sana akasema, “BWANA na abarikiwe leo, ambaye amempa Daudi mwana wa hekiima juu ya kundi hili kubwa.” [8] Hiramu akatuma neno kwa Sulemani, akisema, “Nimeupata ujumbe ule ulionitumia. Nitatoa miti yote ya mierezi na miti ya miberoshi ambayo unahitaji. [9] Watumishi wangu wataileta miti kutoka Lebanoni hadi baharini, nami nitaiendesha baharini mpaka mahali utakaponielekeza. Nitaigawa pale, nawe utaichukua. Utafanya kile ninachohitaji kwa kuwapa chakula watumishi wangu.”
[10] Kwa hiyo Hiramu akampa Sulemani miti yote ya mierezi na miti ya miberoshi ambayo alihitaji. [11] Sulemani akampa Hiramu kori ishirini elfu za ngano kwa ajili ya chakula cha watumishi wake na kori ishirii za mafuta safi. Sulemani akavitoa hivi kwa Hiramu mwaka baad ya mwaka. [12] BWANA akampa Sulemani hekima, kama alivyokuwa amemwahidi. Kulikuwa na amani kati ya Hiramu na Sulemani na wote wawili wakafanya agano. [13] Mfalme Sulemani akaandaa wafanya kazi kutoka Israeli yote. Idadi ya watenda kazi walioandaliwa ilikuwa wanaume elfu thelathini. [14] Aliwatuma kwenda Lebanoni, aliwatuma kwa zamu ya watu elfu kumi kila mwezi. Kwa mwezi mmoja walienda Lebanoni na miezi miwili walikaa nyumbani. Adoniramu ndiye aliyekuwa msimamizi wa watenda kazi. [15] Sulemani alikuwa na watu elfu sabini waliokuwa wabeba mizigo na watu elfu themanini wa kukata mawe milimani, [16] zaidi ya hao, walikuwepo maakida 3, 300 ambao pia

waliokuwa wakiisimamia hiyo kazi. [17] Kwa amri ya mfalme walileta mawe makubwa
ya thamani kwa ajili ya kulaza kwenye msingi wa hekalu. [18] Kwa hiyo wajenzi wa
Sulemani na wajenzi wa Hiramu na Wagebaliti walifanya kazi ya kukata na kuandaa
mbao kwa ajili ya ujenzi wa hekalu.

# 6

[1] Kwa hiyo Sulemani akaanza kulijenga hekalu. Hii ilikuwa mwaka wa 480 baada
ya wana wa Israeli kutoka katika nchi ya Misri, katika mwaka wa nne wa utawala
wa Sulemani huko Israeli, katika mwezi wa Ziv, ambao ndio mwezi wa pili. [2] Hekalu
ambalo mfalme Sulemani alimjengea BWANA lilikuwa na urefu wa mita 27, na
upana wa mita 9, na kimo cha mita 13. 5. [3] Na ukumbi uliokuwa mbele ya hekalu
ulikuwa na urefu wa mita 9 na upana wa mita 4. 5 sawa na upana wa sehemu
kuu ya hekalu. [4] Lile hekalu alilitengenezea madirisha ambayo fremu zake kwa nje
yalifanya yaonekane membamba kuliko ile sehemu ya ndani. [5] Na ukuta wa nyumba
aliuzungushia vyumba kuzunguka pande zake, kushikamana na vyumba vya nje na
vya ndani ya hekalu. Akajenga vyumba katika pande zote. [6] Kile chumba cha chini
kilikuwa na upana wa mita 2. 3, kile cha kati kilikuwa na upana wa mita 2. 8. na
kile cha tatu kilikuwa na upana wa mita 3. 2. upande wa nje akaupunguza ukuta
wa nyumba pande zote, ili boriti zisishikamane ukutani mwa nyumba. [7] Hekalu
lilijengwa kwa mawe yaliyokuwa yamechongwa chimboni. Hakuna nyundo, wala
shoka au chombo chochote cha chuma kilisikika wakati hekalu lilipokuwa likjengwa.
[8] Upande wa kusini wa hekalu kulikuwa na lango la chini, ambalo mtu hupanda
kwa madaraja mpaka juu kwenye chumba cha kati, na kutoka chumba cha kati
hadi chumba cha tatu. [9] Kwa hiyo Sulemani akalijenga hekalu mpaka akalimaliza,
akalifunika hekalu kwa boriti na mbao za mwerezi. [10] Akajenga vyumba vya pembeni
mwa hekalu, kila upande mita 2. 3 kwenda juu. Navyo vikaunganishwa na hekalu
kwa mbao za mierezi. [11] Neno la BWANA likamjia Sulemani, likisema, [12] “Kuhusu
hili hekalu ambalo unajenga, kama utatatembea katika maagizo yangu na kuhukumu
kwa haki, na kutunza amri zangu na kuishi kwa hizo, ndipo ntakapozithibitisha ahadi
zangu na wewe ambazo niliziahidi kwa baba yako Daudi. [13] Nitaishi kati ya watu wa
Israeli nami sitawatupa.” [14] Kwa hiyo Sulemani akalijenga hekalu mpaka akalimaliza.
[15] Kisha akajenga kuta za ndani za hekalu kwa mbao za mwerezi. Kuanzia sakafu
ya hekalu hadi boriti za juu, kwa ndani akazifunika kwa miti, na akaifunika sakafu
kwa mbao za miberoshi. [16] Alijenga mita 9 ndani ya hekalu kwa mbao za miberoshi
kutoka sakafuni hadi juu. Hiki ni chumba cha ndani, cha patakatifu sana. [17] Ule
ukumbu mkuu, ulikuwa mahali pakatifu amabao ulikuwa mbele ya patakatifu sana,
ulikuwa wa mita 18. hapo kulikwa na mbao za mwerezi ndani ya hekalu, zilizokuwa
zimechongwa kwa sura ya vibuyu na maua yaliyochanua. [18] Zote zilikuwa za
mierezi kwa ndani. Hapakuonekana chochote ndani kilichokuwa kimetengenezwa
kwa mawe. [19] Sulemani alitengeneza kile chumba cha ndani kwa lengo la kuweka
sanduku la agano la BWANA. [20] Kile chumba cha ndani kilikuwa na upana wa mita
9, na kimo cha mita 9. Sulemani alizifunika kuta kwa dhababu na madhabahu
aliifunika kwa mbao za mierezi. [21] Sulemani alifunika ndani ya hekalu kwa dhahabu
safi na akaweka mikufu ya dhahabu iliyopita mbele ya chumba cha ndani, na
kulifunika eneo la mbele kwa dhababu. [22] Akalisakafia kwa dhahabu eneo lote
la ndani mpaka akamaliza hekalu lote. Pia akalisakafia kwa dhahabu madhahabu
yote ya chumba cha ndani. [23] Sulemani akatengeneza makerubi mawili kwa mbao
za mizeituni, kila moja lilikuwa na kimo cha mita 4. 5 kwa ajili ya chumba cha
ndani. [24] Bawa moja la kerubi wa kwanza lilikuwa na urefu wa mita 2. 3. Kwa
hiyo kutoka ncha ya bawa moja hadi ncha ya bawa lingine kulikuwa na umbali wa

mita 4. 5. Yule [25] kerubi mwingine naye alikuwa na bawa lenye kipimo cha mita
4. 5 Makerubi hawa walikuwa wanafanana kwa umbo na kwa vipimo. [26] Kimo cha
kerubi mmoja kilikuwa mita 4. 5 na yule wa pili alikuwa hivyo hivyo. [27] Sulemani
aliwaweka hao kerubi kwenye chumba cha patakatifu sana. Bawa moja la kerubi
lilikuwa limeenea kiasi kwamba bawa moja liligusa ukuta huu na bawa la yule wa
pili nalo liligusa ukuta wa upande mwingine. Hayo mabawa yalikuwa yanakutana
katikati ya chumba cha patakatifu sana. [28] Sulemani aliwafunika hao kerubi kwa
dhahabu. [29] Akazinakshi kuta zote kwa sura za makerubi, miti ya mitende, na maua
yaliyochanua, kwa vyumba vya nje na vya ndani. [30] Sulemani akalisakafia hekalu
kwa dhahabu, kwa vyumba vyote vya ndani na vya nje. [31] Sulemani akatengeneza
milango ya mbao za mizeituni kwenye lango la kuingia ndani. Aliweka vizingiti na
miimo kwenye pande tano. [32] Kwa hiyo akatengeneza na milango miwili ya mizeituni,
na akainakshi kwa makerubi, na mitende, na maua yaliyochanua. Akasakafia kwa
dhahabu na akatandaza dhahabu kwenye makerubi na kwenye mitende. [33] Kwa
njia hii, akalitengenezea hekalu miimo miwili ya mbao za mizeituni yenye pande
nne [34] na milango miwili ya mbao za mierezi. Zile mbao mbili za mlango mmoja
zilikuwa zikijikunja na mbao mbili za mlango wa pili nazo zilikuwa zikijikunja pia.
[35] Akazinakshi kwa makerubi, mitende, na maua yaliyochanua, na pia akazisakafia
kwa dhahabu juu ya zile nakshi. [36] Akalijengs Korido la ndani kwa safu tatu za mawe
ya kuchongwa na safu moja ya mhimili wa mierezi. [37] Msingi wa hekalu ulijengwa
katika mwaka wa nne, wa mwezi wa Ziv. [38] Mwaka wa kumi na moja mwezi wa Buli,
ambao ndio mwezi wa nane, sehemu zote za hekalu zilimalizika na sharti zake zote.
Sulemani alilijenga hekalu kwa miaka saba.

# 7

[1] Ilimchukua Sulemani miaka kumi na tatu kujenga ikulu yake. [2] Aliijenga ikulu
iliyoitwa mwitu wa Lebanoni. Urefu wake ulikuwa mita 46, na upanawake ulikuwa
mita 23, na kimo chake kilikuwa mita 14. Nayo ilikuwa na safu nne ya nguzo za
mierezi na mithili ya mwerezi juu ya nguzo. [3] Paa la ikulu lilikuwa la mwerezi
ambalo lilikaa juu ya mihimili. Mihili hiyo ilikuwa imeshikiliwa na nguzo. Kulikuwa
na mihimili arobaini na tano, ambayo ilikuwa katika safu kumi na tano. [4] Nayo
mihimili ilikuwa safu tatu, na kila dirisha lilikabili dirisha lingine katika madaraja
matatu. [5] Milango yote na miimo ilitengenezwa kwa mraba, na madirisha yalikuwa
yakikabiliana katika madaraja matatu [6] Akatengeneza baraza lenye uerfu wa mita
23 na upana wa mita 14. Mbele yake kulikuwa na ukumbi ulioezekwa. [7] Sulemani
akajenga baraza yenye kiti cha enzi ambacho alitolea hukumu ya haki. Nayo ilikuwa
imeezekwa kwa mwerezi kutoka sakafu moja hadi nyingine. [8] Nyumba ya Sulemani
ambayo alikusudia kuishi, katika behewa nyingine ndani ya sehemu ya chini ya
ikulu, ilitengenezwa kwa kazi hiyo hiyo. Pia alimjengea binti wa Farao nyumba kama
hii, ambaye alikuwa mke wake [9] Majengo haya yalipmbwa kwa vitu vya thamaini,
mawe ya thamani, yaliyochongwa na kukatwa kwa msimeno kufuata vipimo sahihi
na kulainishwa pande zote. Mawe ya namna hii ndiyo yale yaliyotumika kuanzia
kwenye msingi hadi juu, pia na nje hadi kwenye baraza. [10] Msingi ulijengwa kwa
mawe makubwa sana na ya thamani yenye urefu wa mita 3. 7 na mengine mita
4. 8. [11] Kwa juu ilipambwa kwa, mawe ya thamani yaliyochongwa sawa sawa kwa
msimeno na kwa mihimili ya mierezi. [12] Na behewa kubwa iliyokuwa ikizunguka
ikulu ilikuwa na safu tatu za mawe yaliyokatwa na safu moja ya mihimili ya mierezi
kama ilivyo kwenye baraza la ndani la hekalu la BWANA na ule ukumbi wa hekalu.
[13] Mfalme Sulemani alituma watu kumleta Huramu kutoka Tiro. [14] Huramu alikuwa
mwana wa mjane wa kabila ya Naftali; baba yake alikuwa mtu wa Tiro, mfua shaba.

Huramu alikuwa mwingi wa hekima na ufahamu na stadi za kufanya kazi kubwa
za shaba. Aliletwa kwa mfalme ili kufanya kazi zilizohusiana na shaba kwa mfalme.
15 Huramu alizilemba zile nguzo mbili za shaba, kila moja ilikuwa na kimo cha mita 8.
3 na mzingo wa mita 5. 5. 16 Akatengeneza taji mbili za shaba za kuwekwa juu ya zile
nguzo. Kimo cha kila taji ilikuwa mita 2. 3. 17 Kulikuwa na nyavu za kuwa kama kazi
ya kusuka, na masongo ya mikufu, kwa ajili ya kuvipamba vile vichwa vya nguzo,
nayo yailikuwa saba kwa kila kichwa. 18 Kwa hiyo Huramu akafanya safu mbili za
komamanga kuzunguka vile vichwa vya nguzo ili kuvipamba vile vichwa. 19 Zile
taji kwenye vile vichwa vya nguzo za ukumbi zilikuwa zimepambwa kwa maua,
yenye vimo vya mita 1. 8. 20 Hizo taji kwenye hizo nguzo mbili kwenye vichwa
vyake, karibu yake kulikuwa na makomamanga mia mbili yote yakiwa kwenye safu.
21 Alisimamisha nguzo kwenye ukumbi wa hekalu. Ile nguzo ya kuume akaipa jina
la Yakini, na ile ya kushoto akaipa jina la Boazi. 22 Na juu ya zile nguzo kulikuwa
na mapambo kama maua. Hivyo ndivyo zile nguzo zilivyotengenezwa. 23 Tena
akafanya bahari ya kusubu ya, yenye mita 2. 3 kutoka ukingo hadi ukingo, kimo
chake kilikuwa mita 4. 6, mziingo wake ulikuwa mita 13. 7. 24 Na chini ya ile bahari
kulikuwa na vibuyu vilivyoizunguka, vilikuwa vibuyu kumi na nane katika kila mita,
vilivyowekwa katika kila hicho kipande wakati bahari inapokuwa kalibu. 25 Bahari
ikakaa juu ya makisai kumi na mbili, tatu, zilitazama kaskazini, tatu zikitazama
magharibi, tatu zikitazama kusini na tatu zikitazama kaskazini. Ile bahari iliwekwa
juu yao, na pande zao zote za nyuma zilikuwa ndani. 26 Bahari ilikuwa nene kama
upana wa mkono, na ukingo wake ulikuwakama ukingo wa kikombe, kama ua la
yungi huingia bathi elfu mbili za maji. 27 Huramu akatengeneza makalio kumi ya
shaba. Kila kalio lilkuwa na urefu wa mita 1. 8, upana wa mita 1. 8, na kimo
cha mita 1. 3. 28 Hivi ndivyo kazi za makalio zilivyofanywa. Yalikuwa na papi
ambazo zilikaa kati kati ya vipandio, 29 na juu ya papi na vipandio kulikuwa na
simba, makisai, na makerubi. Chini na juu simba kulikuwa na masongo ya kazi ya
kufuliwa. 30 Kila kalio lilikuwa na magurudumu ya shaba na vipini, na pande zake
nne na miguu yake minne ilikuwa na mataruma chini ya birika. Chini ya birika
yalikuweko mataruma ya kusubu yenye masongo katika kila upande. 31 Na kinywa
chake kilikuwa cha kuviringana, chenye upana wa sentimita araobaini na sita, na ile
taji ilikuwa na sentimita ishirini na tatu. Na kinywa chake kilikuwa na nakshi, na
papi zake zilikuwa za mraba, na wala siyo za mvringo. 32 Yale magurudumu mawili
yalikuwa chini ya papi, na mikono ya magurudumu yalikuwa ndani ya makalio.
Kimo cha yale magurudumu kilikuwa sentimeta sitini na tisa. 33 Yale magurudumu
yalikuwa kama ya gari. Mikono yake, na maduara, matindi yake, na vipande vya
ndani vyote vilikuwa vya kusubu. 34 Kulikuwa na mataruma manne katika pande
zake nne za makalio, yaliyokuwa yameshikamanishwa na kalio lenyewe. 35 Juu ya
makalio kulikuwa na duara yenye kina cha sentimita ishirini na tatu, na juu ya
makalio mashikio yake na papi zake zikiwa zimeshikamanishwa. 36 Juu ya mabamba
na papi zake Huramu akachora makerubi, simba, na mitende ambayo ilifunika nafasi
ya juu, nayo ilikuwa imezungukwa na masongo. 37 Alitengeneza makalio kumi kwa
jinsi hii. Yote yalikuwa yametengenezwa kwa kufanana, na yalikuwa ya vipimo
sawa, na sura inayofanana. 38 Huramu akatengeneza birika kumi za shaba. Birika
moja liliweza kubeba bathi arobaini za maji. Kila birika lilikuwa mita 1. 8 toka
birika moja hadi jingine na kulikuwa na birika moja katika kila kalio kati ya yale
kumi. 39 Alitengeneza makalio tano upande wa kusini unaoelekea upande wa hekalu.
Akatengeneza bahari katika upande wa mashariki, ukielekea upande wa kusini wa
hekalu. 40 Huramu akatengeneza birika na koleo na besini la kunyunyizia. Kisha
akamaliza kazi yote aliyofanya kwa mfalme Sulemani katika hekalu la BWANA: 41 Zile

nguzo mbili, na lile besini lakawa kama taji ambalo lilikuwa juu ya zile nguzo, na
nyavu mbili za mapambo za kufunika zile besini mbili za kuwa kama taji zilizokuwa
juu ya nguzo. 42 Kisha akatengeneza makomamanga mia nne kwa ajili ya zile nyavu
mbili za mapambo: safu mbili za makomamamanga kwa kila kazi ya nyavu kwa ajili
ya kufunikia zile besini mbili kama taji iliyo juu ya nguzo, 43 yale makalio kumi, na
birika kumi kwenye makalio. 44 Akatengeneza bahari na makisai kumi chini yake;
45 na masufuria, koleo, birika na vyombo vingine vyote. Huramu akivitengeneza kwa
shaba iliyosuguliwa, kwa ajili ya mfalme Sulemani, na kawa ajili ya hekalu la BWANA.
46 Mfalme alivisubu katika uwanda wa Yorodani, katika udongo mfinyanzi kati ya
Sukoti na Zarethani. 47 Sulemani hakuvipima vyombo vyote kwa sababu vilikuwa
vingi mno kuvipima, na kwa sababu uzito wa shaba ulikuwa hauwezi kupimwa.
48 Sulemani akatengeneza mapambo yote yaliyokuwa kwenye hekalu la BWANA kwa
kutumia dhahabu: Ile madhabahu ya dhahabu na ile meza ambayo iliwekwa mikate
ya wonyesho. 49 Vile vinara vya dhahabu, ambavyo vitano vilikuwa upande wa kulia
na vitano mkono wa kushoto, mbele ya chumba cha ndani, vilikuwa vya dhahabu safi,
na maua, na taa na koleo zilikuwa za dhahabu. 50 Vile vikombe, na makasi, mabakuri,
na vijiko, na vyetezo vyote vilikuwa vimetengenezwa kwa dhahabu safi. na bawaba
za dhahabu za milango ya ndani, ambazoo ndio mahali patakatifu sana, na milango
ya ukumbi mkubwa, vyote vilitengenezwa kwa dhahabu. 51 Kwa njia hii, kazi yote
ambayo mfalme Sulemani alifanya kwa ajili ya hekalu ilimalizika. Kwa Sulemani
akaviingiza ndani yake vitu vile vilivyokuwa vimewekwa wakfu na Daudi, baba yake,
na fedha na dhahabu, na mapambo, na vile vya ndani ya hazina ya BWANA.

# 8

1 Kisha Sulemani akawakusanya wazee wa Israeli, wakuu wote wa makabila, na
viongozi wa familia za wana wa Israeli, mbele yake kuleYerusalemu, ili waliingize
ndani lile sanduku la agano la BWANA kutoka mji wa Daudi, ambao ni Sayuni.
2 Wanaume wote wa Israeli walikusanyika mbele ya mfalme Sulemani kwenye
sherehe, katika mwezi wa Ethanim, ambao ndio mwezi wa saba. 3 Wazee wote wa
Israeli walikuja, na makuhani wakalibeba lile sanduku. 4 Wakalileta lile sanduku
la BWANA, lIle hema la kukutania na mapambo yote matakatifu ambayo yalikuwa
kwenye hema. Makuhani na Walawi wakavileta vitu hivi. 5 Mfame Sulemani na
mkutano wote wa Israeli wakaja pamoja mbele ya sanduku, wakatoa sadaka za
kondoo na makisai ambazo hazikuweza kuhasabika. 6 Makuhani wakalingiza ndani
lile sanduku la agano la BWANA na wakaliweka mahali pake, ndani ya chumba cha
ndani, patakatifu sana, chini ya yale mabawa ya makerubi. 7 Kwa kuwa makerubi
walitandaza mabawa yao hadi mahali pa sanduku la agano, na walifunika sanduku
na miti yake kwani ilitumika kulibeba. 8 Ile miti ilikuwa mirefu sana kiasi kwamba
miishio yake ilionekana tokea kwenye eneo takatifu mbele ya chumba cha ndani,
lakini haikuweza kuonekana kutokea nje. Miti hiyo iko mpaka leo. 9 Ndani ya
sanduku hapakuwemo na kitu chochote isipokuwa vile vidonge vya mawe ambavyo
Musa aliviweka alipokuwa mlima Horebu, wakati BWANA alipofanya agano na watu
wa Israeli walipotoka kwenye nchi ya Misri. 10 Ilitokea kwamba wakati makuhani
walipotoka mahali patakatifu, lile wingu lilifunika hekalu la BWANA. 11 Makuhani
hawakuweza kusimama kwa ajili ya kutumika kwa sababu utukufu wa BWANA
ulifunika hekalu. 12 Kisha Sulemani akasema, “BWANA amsema kuwa anaweza
kuishi hata kwenye giza nene, 13 Lakinni nimekujengea makao ya kujivunia, mahali
pako pa kuishi milele.” 14 Kisha mfalme akageuka na kuwabariki mkusanyiko wa
watu wa Israeli, wakati huo mkusanyiko wa Waisraeli walikuwa wamesimama.
15 Akasema, “BWANA, Mungu wa Israeli, asifiwe, ambaye alisema na baba yangu

Daudi, na ametimiza kwa mikono yake, akisema, [16] 'Tangu siku ile niliyowatoa watu
wangu Israeli kutoka Misri, sikuchagua mji wowote toka kwa makabila yote ya
Israeli ambako ningeijenga nyumba, kwa ajili ya jina langu kuwemo humo. Hata
hivyo, nilimchagua Daudi kuwatawala watu wangu Israeli. [17] Sasa ilikuwa kwenye
moyo wa Daudi baba yangu kujenga nyumba kwa jina la BWANA, Mungu wa Israeli.
[18] Lakini BWANA alimwambia baba yangu Daudi, 'Ilikuwa ndani ya moyo wako
kunijengea nyumba kwa jina langu, ulifanya vyema kwa hilo kuwa ndani ya moyo
wako. [19] Ingawa hutanijengea nyumba; badala yake mwanao, mmoja wa wanao
atakayezaliwa toka viunoni mwako, atanijengea nyumba kwa jina langu,' [20] BWANA
amelibeba lile neno slilokuwa amesema, kwa kuwa nimeinuka mahali pa baba yangu
Daudi, na nimeketi kwenye kiti cha enzi cha Israeli, kama BWANA alivyoahidi.
Nimeijenga nyumba kwa jina la BWANA, Mungu wa Israeli. [21] Nimetengeneza
mahali kwa ajili ya sanduku ndani yake, ambamo ndani yake kuna agano la BWANA,
ambalo alifanya na baba zetu alipowatoa toka nchi ya Misri," [22] Sulemani alisimama
mbele ya madhabahu ya BWANA, mbela ya mkusanyiko wote wa Waisraeli, naye
akanyosha mikono yake kuelekea mbinguni. [23] Akasema, "BWANA, Mungu wa Israeli,
hakuna Mungu kama wewe juu mbinguni au chini duniani, ambaye hutunza agano
lake kwa uaminifu kwa watumishi wako ambao hutembea mbele yako kwa mioyo
yao yote; [24] wewe ambaye umetunza ahadi yako na mtumishi wako Daudi baba
yangu ile uliyomwahidi. Naam, ulisema kwa kinywa chako na sasa umeitimiza kwa
mkono wako, kama ilivyo leo. [25] Sasa basi, BWANA, Mungu wa Israeli, timiza kile
ulichomwahidi mtumishi wako Daudi baba yangu, pale uliposema, 'Hautashindwa
kunipa mtu mbele ya macho yangu ambaye ataketi katika kiti cha enzi cha Israeli,
kama tu uzao wako watakuwa waangalifu kutembea mbele yangu, kama vile wewe
ulivyotembea mbele yangu.' [26] Sasa basi, Mungu wa Israeli, Ninaomba kwamba
ile ahadi uliyofanya kwa mtumishi wako Daudi baba yangu, itimie. [27] Je, ni kweli
kwamba Mungu ataishi duniani? Tazama, Ulimwengu wote na mbingu hazikutoshi -
sembuse nyumba hii niliyoijenga! [28] Kwa hiyo Mungu naomba uyajali maombi haya
ya mtumishi wako na maombi yake, BWANA, Mungu wangu; sikiliza kilio na maombi
ambayo mtumishi wako anakuomba leo. [29] Naomba ulitazame hekalu hili mchana
na usiku, mahali ambapo ulisema, 'Jina langu na uwepo wangu utakuwa' - ili niweze
kuwa nasikiliza maombi ambayo mtumishi wako ataomba mahali hapa. [30] Kwa hiyo
sikia maombi ya mtumishi wako na ya watu wako Israeli tunapokuwa tunaomba
mahali hapa. Ndiyo, sikia kutokea mahali ambapo unaishi, kutoka katika mbingu
za mbingu; na unaposikia tafadhali samehe. [31] Kama mtu atamtendea uovu jirani
yake na anapewa sharti la kiapo, na kama atakuja na kuapa mbele ya madhabahu
yako katika nyumba hii, [32] basi usikie kutoka mbinguni ukatende na kuwahukumu
watumishi wako, ukamhukumu mwovu, ili kuwaletea tabia zake kichwani mwake,
na kumtunza mwenye haki kuwa hana hatia, na kumpa thawabu yake ya haki.
[33] Watu wako Israeli watakapopigwa na adui kwa sabau ya kutenda dhambi dhidi
yako, na kama watakurudia, na kulikiri jina lako, na kukusihi, na kuomba msamaha
kwako katika hekalu hili- [34] tafadhali nakuomba usikie kutoka mbinguni na usamehe
dhambi za watu wako Israeli; uwarudishe katika nchi ambayo uliwapa mababu zao.
[35] Kama mbingu zitafungwa na mvua hazinyeshi kwa sababu watu wamekutenda
dhambi wewe - na kama wataomba mahali hapa, na kulikiri jina lako, na kugeuka
toka dhambi zao na kama umewapiga - [36] basi sikia tokea mbinguni na usamehe
dhambi za watumishi wako na za watu wako Israeli, utakapowafundisha njia njema
inayowapasa; basi uinyeshee mvua nchi yako, ambayo uliwapa watu wako kuwa
urithi. [37] Na kama kuna njaa katika nchi, au kama kuna magonjwa, au ukungu, nzige
au funza; au kama adui atavamia malango ya mji katika nchi yao, kama kuna tauni

au magonjwa yeyote - 38 na kama kuna mtu au wata wa Israeli wataomba - kila mmoja
akaijua hiyo tauni katika moyo wake wakati akinyosha mikono yake katika hekalu
hili. 39 Basi usikie kutoka mbinguni, mahali unapoishi, utende na kusamehe, na umpe
kila mtu thawabu anayostahili kwa kile anachofanya; wewe unajua moyo wake, kwa
sababu ni wewe pekee yako ujuaye mioyo ya watu. 40 Fanya hivi ili kwamba wawe na
hofu kwako katika siku zote za maisha yao wanayoishi katika nchi uliyowapa mababu
zetu. 41 Na nyongeza yake, kuhusiana na mgeni ambaye si mtu wako wa Israeli:
atakapokuja kutokea nchi ya mbali kwa sababu ya jina lako - 42 kwa sababu watasikia
jina lako lilivyo kuu, mkono wako wenye nguvu, na mkono wako ulioinuliwa -
atakapokuja na kuomba mahali hapa pa hekalu, 43 tafadhali usikie kutokea katika
mbingu, mahali unapoishi, na umfanyie huyo mgeni akuombacho. Fanya hivi ili
makundi ya wtu wote duniani wakujue jina lako na kukuhofia, kama wanavyofanya
watu Israeli. Fanya hivyo ili wajue kwamba nyumba hii niliyoijenga inaitwa kwa
jina lako. 44 Na kama watu wko wataenda vitani dhidi ya adui, kwa njia yeyote
unayoweza kuwatuma, na kama watakuomba wewe, BWANA, kuelekea mji huu
uliuchagua, na kuekea nyumba ambayo nimeijenga kwa jina lako. 45 Basi sikia tokea
mbinguni maombi yao, dua zao, na uwasaidie wanachohitaji. 46 Na kama watafanya
dhambi dhidi yako, kwa kuwa hakuna hata mtu mmoja asiyefanya dhambi, na kama
una hasira dhidi yao na kuwapeleka kwa maadui, ili kwamba maadui wawachukue
mateka katika nchi yao, mbali au karibu. 47 Na kama watatambua kuwa wako katika
nchi ya utumwa, na kama watatubu na kuomba neema kwako kutokea katika nchi
ya watekaji. Na kama watasema, 'tumetenda kwa ukaidi na tumefanya dhambi.
Tumetenda kwa uovu.' 48 Na kama watarudi kwako kwa mioyo yao yote na kwa
roho zao zote katika chi ya maadui ambao wanawakamata, na kama watakuomba
wewe kuelekea nchi yao, ambayo uliwapa mababu zao, na kuelekea katika mji
uliouchagua, nakuelekea kaika nyumba ambayo nimeijenga kwa jina lako. 49 Basi
usikie maombi yao, na dua zao tokea mbinguni, mahali unapoishi, na ukaitetee haki
yao. 50 Wasamehe watu wako waliotenda dhambi dhidi yako, na dhambi zao zote
ambazo kwazo wamekukosea wewe dhidi ya amri zako. Uwahurumie mbele ya
maadui zao ambao waliwachukua mateka, ili kwamba maadui zao pia wawahurumie
watu wako. 51 Hawa ni watu wako uliowachagau, ambao uliwaokoa toka nchi ya
Misri kama kwamba walikuwa katikati ya tanuru amabamo vyuma huyeyushwa.
52 Naomba kwamba macho yako yatazame dua za mtumishi wako na kwa dua
za watu wako Issraeli, ili uwasike kila wanapokulilia. 53 Kwa kuwa uliwatenga
toka kwa watu wengine wa duniani ili wawe wako nakupokea ahadi zako, kama
vile ulivyomwambia Musa mtumishi wako, wakati ulipowatoa babazetu toka Misri,
BWANA." 54 Kwa hiyo ilitokea wakati Sulemaeni alipomaliza kuomba maombi haya
na dua zake kwa BWANA, aliamka toka madhabahu ya BWANA, pale alipokuwa
amepiga magoti na mikono yake ikiwa imenyoshwa kuelekea mbinguni. 55 Alisimama
na kuubariki mkutano wote wa Israeli kwa sauti kuu, alisema, 56 "Asifiwe BWANA,
aliywapatia pumziko watu hawa Israeli, akitunza ahadi zake zote. Hakuna hata moja
ambayo haijatekelezwa katika ahadi njema za BWANA ambazo aliahidi akiwa na
Musa mtumishi wake. 57 BWANA, mungu wetu awe pamoja nasi, kama alivyokuwa
pamoja na mababu zetu. Asituache wala kututelekeza, 58 kwamba aunganishe mioyo
yetu na yeye, ili tuishi katika njia zake na kuzishika amri zake na taratibu zake na
maagizo yake, ambayo aliwaagiza baba zetu. 59 Na maeneo haya ambayo nimesema,
ambayo nimesihi mbele ya BWANA, yawe karibu n a BWANA, Mungu wetu usiku
na mchana, ili kwamba awasadie katika haki za mtumishi wake na haki za watu
wake Israeli, kama watakavyoomba kila siku; 60 kwamba watu wote duniani wajue
kwamba BWANA, ndiye Mungu, na hakuna Mungu mwingine! 61 Kwa hiyo ifanyeni

mioyo yenu iwe ya haki mbele ya BWANA. Mungu wetu, ili tutembee katika maagizo
na kuzishika amri zake, kama ilivyo leo. 62 Kwa hiyo mfalme na watu wote pamoja
naye wakatoa sadaka kwa BWANA. 63 Sulemani akatoa sadaka ya amani, ambayo
aliifanya kwa BWANA: Nayo ilikuwa makisai elfu ishirini na mbili, na kondoo 120,
000. Kwa hiyo mfalme na watu wa Israeli wakaiweka wakfu nyumba ya BWANA.
64 Siku hiyo mfalme aliweka wakfu behewa ya katikati mbele ya hekalu la BWANA,
kwa kuwa pale ndipo alipotoa sadaka za kuteketezwa, sadaka za unga, na sadaka za
mafuta ya amani, kwa sababu ile madhabahu ya shaba iliyokuwa mbele ya BWANA
ilikuwa ndogo sana kwa sadaka za kuteketezwa, sadaka za unga, na mafuta ya sadaka
za amani. 65 Kwa hiyo Sulemani akafanya sherehe wakati huo, Nayo Israeli yote
pamoja naye, mkutano mkubwa, kutoka Lebo Hamathi hadi kijito cha Misri, wakaja
mbele ya BWANA, Mungu wetu kwa muda wa siku saba na pia kwa siku saba zingine,
ambayo jumla yake ni siku kumi na nne. 66 Na ilipofika siku ya nane aliwatawanya
watu, nao wakambariki mfalme kisha wakaenda nyumbani kwao kwa furaha na
mioyo ya shangwe kwa wema wote ambao BWANA alimwonyesha Daudi, mtumishi
wake, na kwa watu wake, Israeli.

# 9

1 Sulemani alipomaliza kulijenga hekalu la BWANA, na ikulu ya mfalme, na baada
ya kukamilisha vyote alivyokusudia kufanya, 2 BWANA alionekana kwa Sulemani kwa
mara ya pili, kama alivyoonekana kwake kule Gibeoni. 3 Na BWANA akamwambia,
“ Nimeyasikia maombi yako na dua zako ambazo umeniomba. Nimeitakasa nyumba
hii ambayo umeijenga, kwa ajili yangu, ili niweke jina langu humo milele. Macho
yangu na moyo wangu yatakuwa humo kwa nyakati zote. 4 Lakini pia na wewe, kama
utatembea mbele zangu kama Daudi baba yako alivyotembea kwa haki na unyofu
katika moyo wako, ukitii yote niliyokuamuru na kuyashika maagizo na sheria zangu,
5 ndipo nitakapoimarisha kiti cha enzi kwa Israeli milele, kama nilivyomwahidi
baba yako Daudi, nikiseama, 'uzao wako hautaondoka katika kiti cha enzi cha
Israeli. 6 Lakini kama utageuka, wewe au watoto wako, na kutozishika amri zangu
na maagizo yangu ambayo nimeyaweka mbele zako, na kama utaenda kuabudu
miungu mingine na kuisujidia, 7 basi nitaikatilia mbali Israeli kutoka katika ardhi
niliyowapa; na nyumba hii niliyoitakasa kwa jina langu, nitaitupilia mbali na macho
yangu, na Israeli itakuwa mfano wa kukejeliwa na kitu cha kutusiwa katika mataifa
yote. 8 Ijapokuwa hekalu hili limetukuka sasa, kila mtu atakayepita pembeni yake
atasituka na kuzoomea. Watajiuliza, 'Kwa nini BWANA amefanya hili katika chi hii
na kwa nyumba hii?' 9 Na wengine watajibu, 'Ni kwa sababu walimwacha BWANA,
Mungu wao, ambaye aliwaleta mababu zao toka Misri, na sasa wamegeukia miungu
mingine ambayo wameiinamia na kuisujudu. Hiyo ndiyo sababu BWANA amewaletea
majanga haya yote.” 10 Ilitokea mwishoni mwa miaka ishirini, Sulemani alikuwa
amemaliza kuyajenga majengo yote mawili, hekalu la BWANA na ikulu ya mfalme.
11 Basi Hiramu, mfalme wa Tiro, alikuwa amemletea Sulemani mbao za mierezi
na miboreshi, pamoa na dhahabu; vitu vyote ambavyo Sulemani alitamani. Kwa
hiyo mfalme Sulemani akampatia Hiramu miji ishirini huko Galilaya. 12 Hiramu
akaja kutoka Tiro kuiona ile miji ambayo Sulemani alikuwa amempatia, lakini
hakupendezwa nayo. 13 Kwa hiyo Hiramu akasema, “Ndugu yangu, ni miji gani
hii uliynipatia? Hiramu akaiita nchi ya Kabuli mpaka leo. 14 Hiramu alikuwa
amemtumia mfalme tani nne za dhahabu. 15 Vifuatavyo ndivyo vigezo ambavyo
mfalme Sulemani aliweka: ili kulijenga hekalu la BWANA na ikulu yake, kuijenga
Milo na ukuta wa Yerusalemu, na Hazori, Megido, na Gezari. 16 Farao mfalme wa
Misri alikuwa ameenda kuitwaa Gezeri, akaichoma moto, na kuwaua Wakanaani

katika mji. Kisha Farao akampatia binti yake ule mji, mke wa Sulemani kuwa
zawadi ya arusi. [17] Kwa hiyo Sulemani akaijenga Gezeri na Bethi Horoni ya Loweri,
[18] Baalathi na Tamari jangwani katika nchi ya Yuda, [19] na miji yote ya hazina yote
iliyokuwa yake, na miji ya magari yake, na miji ya wapanda farasi wake, na hata
kama alipenda kuijenga kwa ajili ya fahari yake kule Yerusalemu, Lebanoni, na katika
nchi yote kwenye utawala wake. [20] Na kwa watu wote waliokuwa wamesalia wa
Waamori, Wahiti, Waperezi, Wahivi, na Yebu, ambao hawakuwa Waisraeli, [21] na uzao
wao waliokuwa wamesalia baada yao katika nchi, ambao Waisraeli hawakuweza
kuwaangamiza kabisa - Sulemani akawafanya kuwa vibarua, ambao wako hata leo.
[22] Hata hivyo, Sulemani hakuwafanya kuwa shokoa watu wa Israeli. Badala yake,
walifanyika kuwa wanajeshi wake na watumishi wake, maakida wake, na wakuu
wake, na majemedari wake na wapanda farasi wake. [23] Hawa ndio waliokuwa
maakida wakuu waliokuwa wakiwasimamia kazi za Sulemani, watu 550, walikuwa
wasimamizi wa watu waliokuwa wakifanya kazi. [24] Binti wa Farao alihama kutoka
mji wa Daudi kwenda kwenye ile nyumba ambayo Sulemani alimjengea. Baadaye,
Sulemani akaijenga Milo. [25] Mara tatu kwa kila mwaka Sulemani alitoa sadaka za
kuteketezwa na sadaka za amani katika madhabahu ambayo alimjengea BWANA,
akifukiza uvumba pamoja nazo juu ya madhabahu ilyokuwa mbele ya BWANA. Kwa
hiyo akalimalizia hekalu na sasa alikuwa akilitumia. [26] Tena Sulemani alitengeneza
merikebu kule Ezioni Geberi, ambayo iko karibu na Elathi katika ufukwe wa bahari
ya shamu, katika nchi ya Edomu. [27] Hiramu alituma watumishi kwenye merikebu
ya Sulemani, wanamaji wanaoijua bahari, pamoja na watumishi wake Sulemani.
[28] Walikwenda kwa Ofri pamoja na watumishi wa Sulemani. Kutoka huko walileta
takribani tani 14. 5 za dhahabu kwa Sulemani.

# 10

[1] Malkia wa Sheba aliposikia uvumi wa Sulemani kuhusu jina la BWANA, alikuja
kumjaribu kwa maswali magumu. [2] Alikuja Yerusalemu na msafara mrefu, pamoja na
ngamia waliokuwa wamebeba mizigo ya manukato, dhahabu nyingi, na mawe mengi
ya thamani, akamwambia Sulemani yote yaliyokuwa moyoni mwake. [3] Sulemani
akajibu maswali yake yote. Hapakuwepo na swali ambalo aliuliza na mfalme
akashindwa kujibu. [4] Malkia wa Sheba alipoona hekima yote ya Sulemani, na
ikulu aliyokuwa amejenga, [5] chakula cha mezani kwake, kuketi kwa watumishi
wake, kazi ya watumishi wake na kuvaa kwao, pia wanyweshaji wake, na jinsi
alivyotoa sadaka za kuteketezwa katika nyumba ya BWANA, roho yake ilizimia.
[6] Akamwambia mfalme, “Ni kweli, ile taarifa ambayo nimeisikia nchini kwangu
juu ya maneno yako na hekima yako. [7] Sikuamini kile nilichosikia hadi nilipofika
hapa, na sasa macho yangu yamejionea. Hata nusu ya hekima na utajiri wako!
Umezidi uvumi ambao nilikuwa nimesikia. [8] Tazama jinsi walivyobarikiwa wake
zako, na jinsi walivyobarikwa watumishi wako ambao daima husimama mbele
yako, kwa sababu wanasikia hekima zako. [9] BWANA, Mungu wako asifiwe, ambaye
amependezwa na wewe, ambaye alikuweka kwenye kiti cha enzi cha Israeli. Kwa
sababu BWANA aliipenda Israeli milele, na sasa amekufanya wewe kuwa mfalme,
ili kwamba utoe hukumu ya kweli na ya haki. [10] Basi Malikia alimpatia mfalme
zaidi ya kilo 4500 za dhahabu na kiasi kikubwa cha mawe ya thamani. Hapakuwahi
kutokea kiasi kikubwa cha viungo kama hiki ambacho Malkia wa Sheba alitoa kwa
mfalme Sulemani kuwahi kutolewa tena. [11] Ile merikebu ya Hiramu, ambayo ilileta
dhahabu kutoka Ofri, pia ilileta Kutoka Ofri kiasi kikubwa cha miti ya msandali
na vito vya thamani. [12] Mfalme alitengeneza nguzo za hekalu kwa ajili ya hekalu
la BWANA na kwa nyumba ya mfalme, na vinubi na vinanda kwa hao waimbaji.

haijatokea kiasi cha miti ya misandali kama hicho ambacho kimewahi kutokea hadi
leo. 13 Mfame Sulemani alimpatia Malkia wa Sheba kila kitu ambacho alihitaji,
na kila kitu alichoomba, na zaidi ya yote Sulemani alimpatia kwa ukarimu wake
vitu vya kifalme. Kisha akarudi kwake na watumishi wake. 14 Kiasi cha dhahabu
ambazo zililetwa kwa Sulemani kwa mwaka mmoja kilikuwa takribani kilo elfu
ishirini na tatu za dhahabu, 15 zaidi ya dhahabu ambazo wafanya biashara na
wachuuzi walileta. Wafame wote wa Uarabuni na maliwali wa nchi pia walileta
dhahabu na fedha kwa Sulemani. 16 Mfalme Sulemani alitengeneza ngao mia mbili
za dhahabu iliyofuliwa, shekeli mia sita za dhahabu zilichukuliwa pamoja na ngao.
17 Pia alitengeneza ngao mia tatu za dhahabu iliyofuliwa. Mane tatu za dhahabu
ziliambatana pamoja na ngao moja moja; mfalme aliviweka katika ikulu ya mwitu
ya Lebanoni. 18 Kisha mfalme akafanya kiti kikubwa cha enzi kwa pembe na
akakisakafia kwa dhahabu laini. 19 Hicho kiti kilikuwa na ngazi sita, na kitako
chake kilikuwa cha mviringo. Na kilikuwa kimezungushiwa kwa mikono pande
zake zote. Na simba wawili walisimama pembeni mwa ile mikono. 20 Kulikuwa na
simba kumi na wawili waliokuwa wamesimama kwenye ile ngazi. Moja katika kila
upande wa ngazi hizo. Hapakuwepo na kiti kama hicho katika ufalme mwingine.
21 Vikombe vyote vya kunywea vya mfalme Sulemani vilikuwa vya dhahabu. Na
vikombe vyote vya kunywea vya ikulu ya mwitu wa Lebanoni vilikuwa vya dhahabu
safi. Hapakuwepo na kikombe cha fedha, kwa sababu fedha haikuwa na thamani
katika siku za Sulemani. 22 Mfalme alikuwa na merikebu za kusafiri pamoja na
merikebu za Hiramu. Mara moja kila mwaka merikebu zilileta dhahabu, fedha, na
pembe za ndovu, pamoja na nyani na tumbili. 23 Kwa hiyo mfalme Sulemani aliwazidi
wafalme wote ulimwenguni katika utajiri n a hekiima. 24 Dunia yote ilitafuta uwepo
wa Sulemani ili kusikia hekima yake, ambayo Mungu alikuwa ameweka katika moyo
wake. 25 Na wote waliomtembelea walilipa Kodi, vyombo vya fedha na vya dhahabu,
na nguo na manukato na silaha na farasi na nyumbu, mwaka baada ya mwaka.
26 Sulemani alikusanya pamoja magari n a wapanda farasi. Alikuwa na magari 1,
400 na wapanda farasi elfu kumi na mbili ambao alikuwa amewaweka kwenye miji
ya magari pamoja naye Yerusalemu. 27 Mfalme alikuwa na fedha kule Yerusalemu,
pamoja na mawe ardhini. Alitengeneza miti ya mierezi kuwa mingi kama mikuyu
iliyo katika nyanda za chini. 28 Sulemani alimiliiki farasi waliokuwa wamenunuliwa
kutoka Misri na Kilikia. Wachuuzi wa mfalme waliwanunua kwa makundi, kila kundi
kwa bei yake. 29 Magari yalinunuliwa kutoka Misri kwa shekeli mia sita za fedha kila
moja, na farasi kwa shekeli 150 kila moja. Vitu vingi katika hivi baadaye viliuzwa
kwa wafalme wote wa Wahiti na Aramu.

# 11

1 Basi mfalme Sulemani aliwapenda wanawake wengi wa kigeni: binti wa Farao
na wanawake wa Wamoabu, Waamori, Waedomu, Wasidoni, na Wahiti - Haya
na 2 mataifa ambayo BWANA alikuwa amewaambia Waisraeli kwamba, “Msiwaoe,
wala binti zenu kuolewa nao, kwani kwa hakika wataigeuza mioyo yenu ili mfuate
miungu yao.” Lakini Sulemani aliwapenda wanawake hao. 3 Sulemani alikuwa na
wanawake halali mia saba na masuria mia tatu. Wake zake waliugeuza moyo wake.
4 Kwa kuwa Sulemani alipozeeka, wake zake waliugeuza moyo wake kwa miungu
mingine; hakuutoa moyo wake wote kwa BWANA, Mungu wake, kama ulivyokuwa
moyo wa Daudi baba yake. 5 Kwani Sulemani alimfuata Ashtoreth, mungu mke wa
Wasidoni, na alimfuata Milkom, ambayo ni sanamu chukizo ya Waamori. 6 Sulemani
akafanya maovu mbele ya BWANA; hakumfuata BWANA kwa moyo wake wote, kama
alivyofanya Daudi baba yake. 7 Kisha Sulemani akajenga mahali pa juu pa Kemoshi,

ambayo ni sanamu chukizo ya Wamoabu, mashariki mwa Yerusalemu juu ya kilima,
na vivyo hivyo na Moleki, Sanamu chukizo ya Waamoni. 8 Na kadhalika ndivyo
alivyowafanyia wake zake wa kigeni, ambao walifukiza uvumba na kutoa sadaka
kwa miungu yao. 9 BWANA alichukizwa na Sulemani, kwa sababu moyo wake
ulikuwa umemwacha Mungu wa Israeli, ingawa alikuwa amejionyesha kwake mara
mbili 10 na kumwamuru juu ya mambo haya, kwamba asiwaendee miungu wengine.
Bali Sulemani hakutii kile ambacho BWANA alikuwa amemwamuru. 11 Kwa hiyo
BWANA akamwambia Sulemani, "Kwa kuwa umeyafanya haya haukulishika agano
langu na maagizo ambayo nilikuamuru, basi nitaugawa ufalme kutoka kwako na
kuwapatia watumishi wako. 12 Hata hivyo, kwa ajili ya Daudi, sitalifanya hilo wakati
wa uhai wako, bali nitaugawa wakati ukiwa chini ya mwanao. 13 Bado sitaugawanya
ufalme wote; Nitampa mwanao kabila moja kwa ajili ya Daudi mtumishi wangu,
na kwa ajili ya Yerusalemu, ambayo nimeichagua." 14 Kisha BWANA akamwinulia
uadui Sulemani, Hadadi Mwedomu. Alikuwa anatoka kwenye familiia ya mfalme wa
Edomu. 15 Daudi alipokuwa Edomu, Yoabu mkuu wa jeshi alikuwa ameenda kuzika
mfu, kila mtu aliyekuwa ameuawa kule Edomu. 16 Yoabu na Israeli yote walibaki
huko kwa miezi sita mpaka alipokuwa amewaua wanaume wote wa Edomu. 17 Lakini
Hadadi alichulukuliwa na Waedomu wengine na watumishi wa baba yake hadi Misri,
kuanzia Hadadi alipokuwa mtoto mdogo. 18 Waliondoka Midiani wakaja Parani,
ambapo walichukuliwa na wanaume mpaka Misri, kwa Farao wa Misri, ambaye
alimpa nyumba na ardhi yenye chakula. 19 Hadadi alipata neema kubwa machoni
pa Farao, kwa hiyoFarao akampatia mke, umbu wa mke wake mwenyewe, umbu
la Tapenesi aliyekuwa Malkia. 20 Naye huyo umbu la Tapenesi alimzalia Hadadi
mwana. Wakamwita jina lake Genubathi. Tapenesi akamlea katika ikulu ya Farao.
Kwa hiyo Genubathi alikulia kwenye ikulu ya Farao pamoja na watoto wa Farao.
21 Naye alipokuwa huko Misri, Hadadi alisikia kuwa Daudi alishalala na mababu zake
na kwamba Yoabu mkuu wa majeshi alishakufa, Hadadi akamwambia Farao, "Acha
niondoke nirudi nchini kwangu." 22 Lakini Farao alimwambia, "Umepungukiwa nini
kwangu, kwamba sasa unatafuta kurudi nchini kwako?" Naye Hadadi akamjibu,
"Hapana kitu lakini tafadhali niache niende." 23 Pia Mungu akamwinulia Sulemani
adui mwingine, Rezoni mwana wa Eliada, aliyekuwa amemkimbia bwana wake
Hadadezeri mfalme wa Soba. 24 Rezoni alijikusanyia wanaume naye akawa mkuu
wa jeshi dogo, Daudi ali[owapiga wanaume wa Soba. Wale wanume Rezoni walienda
Dameski kuishi huko, na Rezoni aliitawala Dameski. 25 Yeye akawa adui wa Israeli
katika siku zote za mfalme Sulemani, zaidi ya madhara ambayo Hadadi alisababisha.
Rezoni akawachukia Israeli na akawa juu ya Shamu 26 Kisha Yeroboamu mwana
wa Nebati, mwefraimu wa Sereda, akida wa Sulemani, ambaye jina la mama yake
lilikuwa Serua, mjane, pia akainua mkono wake dhidi ya mfalme. 27 Kisa cha
kuinua mkono wake kinyume cha mfalme ilikuwa ni mfalme Sulemani kujenga Milo
na kufunga mahali palipobomoka katika mji wa Daudi baba yake. 28 Yeroboamu
alikuwa mtu hodari na shujaa. Sulemani akaona kuwa huyo kijana alikuwa na
bidii, kwa hiyo akampa kuwa na mamlaka juu ya wafanyakazi katika nyumba ya
Yusufu. 29 Wakati huo, Yeroboamu alipokuwa akitoka katika Yerusalemu, nabii Ahiya
Mshilo akamkuta barabarani. Sasa Ahiya alikuwa amevaa vazi jipya na kwamba
hawa wawili walikuwa pekee yao kondeni. 30 Kisha Ahiya akalishika lile vazi jipya
ambalo alikuwa nalo na akalichana katika vipande kumi na viwili. 31 Akamwambia
Yeroboamu. "Chukua vipande kumi, kwani BWANA, Mungu wa Israeli, anasema,
'Tazama, Nitaugawa ufalme toka katika mkono wa Sulemani nami nitakupa makabila
kumi. 32 (lakini Sulemani atabaki na kabila moja, kwa ajili ya mtumishi wangu
Daudi na kwa ajili ya mji wangu Yerusalemu - mji ambao nimeuchagua toka kwenye

kabila zote za Israeli), 33 kwa kuwa ameniacha na kumwabudu Ashtorethi mungu
mke wa Wasidoni, Kemoshi Mungu wa Wamoabu, na Milikomu mungu wa watu wa
Amoni. Wameziacha njia zangu, hawakufanya kilicho chema katika macho yangu,
wala hawa kuzishika amri na maagizo yangu, kama alivyofanya Daudi baba yake.
34 Hata hivyo. Stauchukua ufalme wote toka kwenye mkono wa Sulemani. Badala
yake, nimemfanya kuwa mtawala katika siku zake zote za uhai wake, kwa ajili ya
Daudi mtumishi wangu ambaye nilimchagua, mtu ambaye alizishika amri na maagizo
yangu. 35 Bali nitauchukua ufalme ukiwa chini ya mkono wa mwanae na nitakupa
wewe, makabila kumi. 36 Nitampa kabila moja mwana wa Sulemani ili kwamba
Daudi mtumishi wagu atabaki kuwa nuru mbele yangu huko Yerusalemu, mji ambao
nimeuchagua ili niweke jina langu. 37 Nami nitakuchukua, nawe utatawala ili
kutimiza haja yako, nawe utakuwa mfalme juu ya Israeli. 38 Kama utasikiliza yote
ninayokuagaza, na kama utatembea katika njia zangu na kufanya kinachopendeza
mbele ya macho yangu, ukayashika maagizo na amri zangu, kama Daudi mtumishi
wangu alivyofanya, ndipo nitakapokuwa na wewe na nitakujengea nyumba ya
uhakika, kama niliyomjengea Daudi, nami nitakupa Israeli. 39 Nitawaadhibu uzao wa
Daudi, lakini si milele." 40 Kwa hiyo Sulemani akajaribu kumwua Yeroboamu. Lakini
Yeroboamu akaamka na kukimbilia Misri, Kwa Shishaki mfalme wa Misri, naye
akabaki Misri mpaka Sulemani alipokufa. 41 Na kwa mambo mengine yanayomhusu
Sulemani, Yote ambayo alifanya na hekima zake, je, hayakuandikwa katika kitabu
cha matukio ya 42 Sulemani? Sulemani alitawala Yerusalemu juu ya Israeli yote kwa
miaka arobaini. 43 Naye akalala na mababu zake na alizikwa katika mji wa Daudi
baba yake. Rehoboamu mwanae akawa mfalme mahali pake.

# 12

1 Rehoboamu akaenda Shekemu, kwa kuwa Israeli yote walikuwa wameenda
Shekemu kumfanya awe mfalme. 2 Ikatokea kuwa Yeroboamu mwana wa Nebati
akayasikia haya (Kwa kuwa alikuwa bado yuko Misri, ambako alikuwa amekimbilia
kumkwepa mfalme Sulemani), Kwani Yeroboamu alikuwa anaishi Misri. 3 Kwa hiyo
wakatuma watu kumwita, na Yeroboamu pamoja na mkutano wote wa Israeli wakaja
wakamwambia Rehoboamu, 4 Baba yako aliifanya nira yetu kuwa nzito. Sasa ifanye
kazi ngumu ya baba yako kuwa nyepesi kuliko nira ngumu ambayo baba yako
alituwekea, nasi tutakutumikia." 5 Naye Rehobiamu akawaambia, "Ondokeni kwa
siku tatu, kisha nirudieni." Kwa hiyo watu wakaondoka. 6 Mfalme Rehoboamu
akatafuta ushauri kwa wazee waliokuwa wamesimama mbele ya Sulemani baba yake
wakati wa uhai wake, naye akasema, "mnanishauri niwajibuje hawa watu?" 7 Nao
wakamwambia, "Kama wewe utakuwa mtumishi wa hawa watu na akawatumikia,
na akawapa majibu ya maneno mema, ndipo watakapokuwa watumishi wako
daima." 8 Lakini Rehoboamu akapuuzia ushauri aliopewa na wazee na akaenda
kuomba ushauri kwa vijana ambao alikua pamoja nao wakasimama mbele yake.
9 Akawaambia, "Mnanipa ushauri gani ili niweze kuwajibu hawa watu waliosema
nami kwamba, 'ifanye nyepesi nira ambayo baba yako alituwekea'" 10 Wale vijana
waliokua pamoja na Rehoboamu wakamjibu, wakisema, "Waambie hawa watu kuwa
baba yako Sulemani aliifanya nira yenu kuwa nzito lakini ninyi wenyewe mnaweza
kuifanya rahisi. Uwaambie hivi, 'Kidole changu kidogo ni kinene kuliko kiuno
cha baba yangu. 11 Kwa hiyo sasa, ingawa baba yangu aliwatwika kongwa zito,
Mimi nitaiongeza kongwa lenu. Baba yangu aliwaadhibu kwa mijeredi, Lakini
mimi nitawaadhibu kwa nge.'" 12 Kwa hiyo siku ya tatu Yeroboamu na watu
wote wakaja kwa Rehoboamu, kama mfalme alivyokuwa amewaelekeza aliposema,
"mrudi kwangu siku ya tatu." 13 Naye mfalme akawaambia wale watu kwa ukali

na akapuuzia ushauri wa wale wazee ule waliokuwa wamempatia. 14 Akawaambia
akifuata ushauri wa wale vijana; akasema, “Baba yangu aliwatwika kongwa zito,
lakini mimi nitaongeze kongwa lenu. Baba yangu aliwaadhibu kwa mijeredi, mimi
nitawaadhibu kwa nge.” 15 Kwa hiyo mfalme hakuwasikiliza wale watu, kwa kuwa
ilikuwa zamu ya tukio lililoletwa na BWANA, ili kwamba aweze kulitimiza neno
lake ambalo alikuwa amelisema kupitia Ahiya. 16 Israeli yote ilipoona kuwa mfalme
hakuwasikiliza, watu wakamjibu wakimwambia, “Je, tuna sehemu gani kwa Daudi?
Hatuna urithi kwa mwana wa Yese! Nenda kwenye hema zako, ewe Israeli. Sasa
tazama kwenye nyumba yako, Daudi.” Kwa hiyo Israeli akarudi kwenye hema zake.
17 Lakini kwa watu wa Israeli waliokuwa wakiishi kwenye miji ya Yuda, Rehoboamu
akawa mfalme juu yao. 18 Kisha mfalme Rehoboamu akamtuma Adoramu, aliyekuwa
juu ya shokoa, lakini Waisraeli wote wakampiga kwa mawe wakamwua kwa mawe.
Mflme Rehoboamu akakimbia haraka kwa gari lake kwenda Yerusalemu. 19 Kwa
hiyo Israeli wakawa wapinzani dhidi ya nyumba ya Daudi mpaka leo. 20 Ndipo
Israeli yote waliposikia kuwa Yeroboamu alikuwa amerudi, walimwita kwenye
kusanyiko lao wakamweka kuwa mfalme wa Israeli. Hapakuwepo na mtu aliyeifuata
familia ya Daudi, isipokuwa tu kabila la Yuda. 21 Rehoboamu alipofika Yerusalemu,
akawakusanya wote wa nyumba ya Yuda na kabila la Benjamini; walichaguliwa
wanaume wanajeshi180, 000 ili wapigane na nyumba ya Israeli, kwa lengo la
kurudisha ufalme kwa Rehoboamu mwana wa Sulemani. 22 Lakini neno la Mungu
likamjia Shemaya, mtu wa Mungu; likisema, 23 “Mwambie Rehoboamu mwana wa
Sulemani, mfalme wa Yuda, na kwa nuymba yote ya Yuda na Benjamini, na kwa
watu wote; uwaambie, 24 “BWANA asema hivi, Usipigane wala kuwavamia ndugu
zako watu wa Israeli. Kila mtu lazima arudi nyumbani kwake, kwa kuwa jambo
hili nimelisababisha mimi.” Kwa hiyo wakalisikiliza neno la BWANA na wakrudi
nyumbani kwa njia zao na wakalitii neno lake. 25 Kisha Yeroboamu akaijenga
Shekemu katika nchi ya milima ya Efraimu, na akaishi huko. Akatoka huko na
kuijenga Penueli. 26 Yeroboamu akafikiri moyoni mwake, “Sasa ufalme utarudi
kwenye nyumba ya Daudi. 27 Kama hawa watu wataenda kutoa sadaka kwenye
hekalu la BWANA kule Yerusalemu, basi mioyo ya hawa watu itarudi tena kwa
bwana wao, kwa Rehoboamu mfalme wa Yuda. Wataniua na kurudi kwa Rehoboamu
mfalme wa Yuda.” 28 Kwa hiyo mfalme Yeroboamu akatafuta ushauri na akafanya
ndama wawili wa dhahabu; akawaambia watu, “Ni vigumu sana kwenu kwenda
Yerusalemu. Tazameni, hawa ndiyo miungu yenu, Ee Israeli, iliyowatoa toka nchi
ya Misri.” 29 Akamweka mmoja Betheli na mwingine Dani. 30 Kwa hiyo jambo hili
likawa dhambi. Watu wakaenda kwa huyo na wengine kwa hawa, mpaka huko Dani.
31 Yeroboamu akajenga nyumba mahali pa juu na kufanya makuhani kutoka kwa
watu wote, ambao hawakuwa wana wa Lawi. 32 Yeroboamu akafanya sikukuu katika
mwezi wa nane, katika siku ya kumi na tano ya mwezi, kama sikukuu ambayo iko
Yuda, na akaenda juu kwenye madhabahu. Akafanya hivyo kule Betheli, akawatolea
sadaka wale ndama aliokuwa amewatengeneza, na akaweka kuhani huko Betheli
mahali pa juu alipokuwa amepatengeneza. 33 Yeroboamu akapanda kwenda kwenye
madhabahu ambayo aliitengeneza kule Betheli katika siku ya kumi na tano ya mwezi
wa nane, ndio mwezi aliokuwa amefikiri katika akili yake; akafanya sikukuu kwa
watu wa Israeli n a akaenda madhabahuni kufukiza uvumba.

## 13

1 Mtu wa Mungu alikuja tokea Yuda kwa neno la BWANA kule Betheli. Naye
Yeroboamu alikuwa amesimama karibu na madhabahu ili kufukiza uvumba. 2 Akalia
kinyume na zile madhabahu kwa neno la BWANA: “Ee madhabahu, madhabahu”

hivi ndivyo asemavyo BWANA, 'Tazama, mwana aitwaye Yosia atazaliwa katika
familia ya Daudi, na juu yenu atawachinja makuhani ambao sasa wanafukiza
uvumba mahali hapa pa juu kwa ajili yako. Juu yako watachoma mifupa ya watu.'"
3 Kisha mtu wa Mungu akatoa ishara siku hiyohiyo, akisema, "Hii ndiyo isharaya
kwamba BWANA amesema: 'Tazama, madhabahu zitavuunjika, na majivu yaliyo juu
yatamwagika." 4 Naye mfalme aliposikia kile mtu wa Mungu alichosema, kwamba
amelia kinyume cha zile madhabahu kule Betheli, Yeroboamu akanyosha mkono
wake kutoka madhabahuni, akisema, "mkamateni." Ndipo ule mkono aliokuwa
ameunyosha dhidi ya mtu wa Mungu ukakauka, kiasi kwamba hakuweza kuurudisha
mwenyewe. 5 Na ile madhabahu ikavunjika vipande vipande, na yale majivu
yakamwagika kutoka madhabahuni, kama ilivyokuwa imefafanuliwa kuwa ndiyo
ishara ya kwamba mtu wa Mungu alikuwa amepewa kwa neno la BWANA. 6 Mfalme
Yeroboamu akajibu akimwambia mtu wa Mungu, "Msihi BWANA, Mungu wako akupe
neema ili uniombee, ili kwamba mkono wangu urejee kwangu tena." Kwa hiyo mtu
wa Mungu akamwomba BWANA, na mkono wa mfalme ukarejea katika hali yake
tena, na ukawa kama ulivyokuwa mwanzoni. 7 Yule mfalme akamwambia mtu wa
Mungu, "twende nyumbani kwangu upate chakula, nami nitakupa zawadi." 8 Yule
mtu wa Mungu akamwambia mfalme, "Hata kama utanipa nusu ya miliki yako.
staende na wewe, wala sitakula au kunywa maji mahali hapa, 9 kwa sababu BWANA
ameniamuru kwa neno lake, 'hutakula mkate wala kunywa maji, wala kurudi kwa
njia ulioijia.'" 10 Kwa hiyo mtu wa Mungu akaondoka na hakurudi nyumbani kwa njia
aliyokuja nayo huko Betheli. 11 Sasa kulikuwa na nabii mwingine mzee aliyekuwa
akiishi Betheli, na mmoja wa wana wake akaja kumwambia mambo yote ambayo mtu
wa Mungu amefanya siku hiyo kule Betheli. Wana wake wakamwambia pia maneno
ambayo Yule mtu wa Mungu alimwambia mfalme. 12 Baba yao akawaambia, "Aliendा
kwa njia gani?" Wale wanawe walikuwa wamemwona yule mtu wa Mungu kutoka
Yuda njia aliyotumia kurudi. 13 Kwa hiyo akawaambia wanawe, "Nitandikeni punda."
Kwa hiyo wakamtandikia punda naye akampanda. 14 Yule nabii mzee akamfuata yule
mtu wa Mungu na akamkuta amekaa chini ya mti wa mwaloni; akamwambia, "Je,
wewe ndiye mtu wa Mungu aliyetoka Yuda?" Naye akamjibu, "Mimi ndiye." 15 Kisha
yule nabii mzee akamwambia, "twende nyumbani kwangu ukale chakula." 16 Yule
mtu wa Mungu akamjibu, "Siwezi kurudi na wewe wala kuingia ndani na wewe, tena
sitakula chakula wala kunywa maji pamoja na wewe mahali hapa, 17 kwa sababu
niliamuriwa hivyo kwa neno la BWANA, 'Hautakula chakula wala kunywa maji kule,
wala kurudi kwa njia utakayokuja nayo.'" 18 Kwa hiyo yule nabii mzee akamwambia,
"Mimi pia ni nabii kama ulivyo, na malaika amesema na mimi neno la BWANA,
akisema, 'Mrudishe aje na wewe katika nyumba yako, ili aweze kula chakula na
kunywa maji.'" Lakini alikuwa anamdanganya mtu wa Mungu. 19 Kwa hiyo yule mtu
wa Mungu akarudi pamoja na yule nabii mzee na akala chakula nyumbani kwake na
akanywa maji. 20 Walipokuwa wamekaa mezani, neno la BWANA likamjia yule nabii
aliyemrudisha, 21 naye akalia kwa mtu wa Mungu aliyetoka Yuda, akisema "BWANA
anasema, 'Kwa kuwa umeshindwa kutii nenola BWANA na umeshindwa kuishika
amri ya BWANA ambayo Mungu wako alikupa, 22 bali umerudi na umekula chakula
na kunywa maji mahali ambapo BWANA alikwambia usile chakula wala kunywa
maji, basi mwili wako hautazikwa kwenye makaburi ya baba zako.'" 23 Baada ya
kula chakula na kunywa maji, Yule nabii akatandika punda wa mtu wa Mungu,
yule mtu aliyerudi naye. 24 Baada ya mtu wa Mungu kuondoka, akakutana na
simba njiani na kumwua barabarani, na mwili wake uliachwa barabarani. Na yule
punda akasimama pembeni yake, na yule simba naye akasimama pembeni ya ule
mwili. 25 Watu walipopita na kuuona ule mwili umeachwa barabarani, na yule

simba akisimama karibu na ule mwili, walikuja wakaeleza habari hiyo mjini kule
ambako yule nabii mzee aliishi. [26] Yule nabii aliyemrudisha toka njiani aliposikia,
akasema, “Yeye mtu wa Muugu ndiye aliyeshindwa kutii neno la BWANA. Kwa hiyo
BWANA alimtoa kwa simba, ambaye amemrarua katika vipande vipande na kumwua,
kama vile neno la BWANA lilivyokuwa limemwonya.” [27] Kwa hiyo yule nabii mzee
akawaamnbia wanawe, akisema, “Tandikeni punda wangu,” nao wakamtandikia.
[28] Akaenda akaukuta mwili umeachwa barabarani, punda na simba wamesimama
pembeni ya ule mwili. Yule simba hakuula ule mwili, wala hakumshambulia
yule punda. [29] Yule nabii akauchukua ule mwili wa mtu wa Mungu, akaulaza
juu ya punda, na akaurudisha. Akaja kwenye mji wake kuomboleza na kuuzika.
[30] Akaulaza mwili kwenye kaburi lake, nao wakamwombolezea, wakisema, “Aa!
ndugu yangu!” [31] Kisha baada ya kumzika, yule nabii mzee akawaambia wanawe,
akasema, “Nitakapokufa, mtanizika kwenye kaburi ambalo tumemzika mtu wa
Mungu. Mtalaza mifupa yangu pembeni mwa mifupa yake. [32] Kwa kuwa ule ujumbe
uliosemwa na BWANA, dhidi ya madhabahu kule Betheli na dhidi ya nyumba zote za
mahali pa juu katika mji wa Samaria, hakika yatatokea. [33] Baada ya haya Yeroboamu
hakuuacha uovu wake, aliendelea kuchagua makuhani wa kawaida kwa ajili ya
mahali pa juu kutoka kwa watu wa kila aina. Yeyote ambaye angeweza kutumika
alimtakasa kuwa kuhani. [34] Jambo hili likawa dhambi kwenye familia ya Yeroboamu
na kusababisha familia yake kuangamizwa na kuondolewa kabisa katika uso wa
dunia.

# 14

[1] Wakati huo Abiya mwana wa Yeroboamu akawa mgonjwa sana. [2] Yeroboamu
akamwambia mke wake, “amka ujibadilishe, ili wasikutambue kuwa wewe ndiye
mke wangu, na uende Shilo, kwa sababu nabii Ahiya yuko huko, yeye ndiye
aliyeninea mimi kuwa nitakuwa mfalme juu ya watu hawa. [3] Uchukue mikate
kumi, na kaki na mtungi wa asali, na uende kwa Ahiya. Naye atakuambia
kitakachotokea kwa mtoto.” [4] Mke wa Yeroboamu akafanya hivyo; akaenda Shilo
mpaka kwenye nyumba ya Ahiya. Wakati huo Ahiya alikuwa hawezi kuona, kwa
kuwa macho yake yalikuwa yameishiwa nguvu kwa sababu ya umri wake. [5] BWANA
akamwambia Ahiya, “Tazama mke wa Ahiya anakuja kutafuta kutaka ushauri toka
kwako kuhusiana na mwanae, kwa kuwa ni mgonjwa. Mwambie hivi na hivi,
kwa sababu atakapofika atajifanya kuwa ni mwanamke mwingine.” [6] Naye Ahiya
aliposikia sauti za miguu yake alipokuwa akiukaribia mlango, akasema, “karibu,
mke wa Yeroboamu. Kwa nini unajifanya kuwa mtu mwingine? Nimetumwa
kwako nikiwa na habaari mbaya. [7] Nenda ukamwambia Yeroboamu kwamba
BWANA, Mungu wa Israeli, anasema, 'Nilikuinua kutoka kati ya watu na kukufanya
uwe kiongozi wa watu wangu Israeli. [8] Niliugawa ufalme kutoka kwa Daudi na
kukupa wewe, lakini bado hutaki kuwa kama mtumishi wangu Daudi, ambaye
alizishika amri zangu na kunifuata kwa moyo wake wote, na kufanya kilichokuwa
sawa mbele ya macho yangu. [9] Badala yake, umefanya maovu, zaidi ya wote
waliokutangulia. Umetengeneza miungu mingine, na umetengeneza sanamu za
kuyeyushwa ili kunikasirisha na kunitupa nyuma yako. [10] Kwa hiyo, tazama, Nitaleta
majanga kwenye familia yako; Nitawatupilia mbali watoto wako wote wa kiume
katika Israeli, kama ni mtumwa au ni huru, na nitaiondoa familia yako, kama mtu
anayechoma mavi mpaka yaishe. [11] Yeyote ambaye ni mwanafamilia yako atakayefia
mjini ataliwa na mbwa, na yeyote atakayefia shamabani ataliwa na ndege wa angani,
kwa kuwa Mimi BWANA, nimesema; [12] Kwa hiyo inuka wewe mke wa Yeroboamu,
na uende nyumbani kwako; na mguu wako utakapokanyaga mjini, yule mtoto wa

Abiya atakufa. [13] Na Israeli yote itamwombolezea na kumzika. Ni yeye pekee katika
familia ya Abiya atakayepelekwa makaburini, kwa sababu ni yeye pekee yake kutoka
kwenye nyumba ya Abiya, ambaye BWANA, Mungu wa Israeli alimwona kuwa ni
mwema. [14] Pia BWANA atainua mfalme katika Israeli ambaye ataifutilia mbali familia
ya Yeroboamu katika siku hiyo. Leo ndiyo siku hiyo, sasa hivi. [15] Kwa kuwa BWANA
ataishambulia Israeli kama vile majani yanavyotikiswa majini, na ataing'oa Israeli
katika nchi hii njema ambayo aliwpa mababu. Atawatawanya hata ng'ambo ya Mto
Frati, kwa sababu wamefanya nguzo za Ashera kumkasirisha BWANA. [16] Ataiacha
Israeli kwa sababu ya dhambi ya Yeroboamu, dhambi ambazo ametenda, na kwa
hizo ameifanya Israeli kufanya dhambi. [17] Kwa hiyo mke wa Yeroboamu akainuka
na akaondoka na akaenda mpaka Tirza. Naye alipofika kizingitini kwa nyumba
yake, yule mtoto akafa. [18] Isareli wote wakamzika na kumwombolezea, kama vile
alivyokuwa ameambiwa kwa neno la BWANA ambalo amelisema kupitia mtumishi
wake nabii Ahiya. [19] Na kwa mambo mengine yanayOmhusu Yeroboamu, jinsi
alivyopigana vita na jinsi alivyotawala, tazama yameandikwa katika kitabu cha
matukio ya wafalme wa Israeli. [20] Yeroboamu alitawala kwa miaka ishirini na mbili
naye akalala na babu zake, na Nadabu mwanawe akawa mfalme mahali pake. [21] Sasa
Rehoboamu mwana wa Sulemani alikuwa mtawala wa Yuda. Rehoboamu alikuwa na
umri wa miaka arobaini na moja alipokuwa mfalme, na akatawala kwa miaka kumi
na saba kule Yerusalemu, mji ambao BWANA alikuwa ameuchagua kati ya makabila
yote ya Israeli ili aweke jina lake kule. Jina la mama yake alikuwa Naama Mwamori.
[22] Yuda ikafanya yaliyo maovu mbele ya macho ya BWANA; wakamtia wivu kwa
makosa yao, zaidi ya yote ambayo baba zao walikuwa wamefanya [23] Kwa kuwa
walijijengea wenyewe mahali pa juu, nguzo za mawe, na nguzo za Ashera katika
kila mahali pa juu na katika kila mti wenye majani mabichi. [24] Pia kulikuwepo
na ukahaba wa kipagani katika nchi. Walifanya machukizo yaleyale kama wa
mataifa yale ambayo BWANA alikuwa amewafukuza kutoka kwa watu wa Israeli.
[25] Ilitokea wakati wa mwaka wa tano wa mfalme Rehoboamu wakati Shishaki akiwa
mfalme wa Misri, akaja kinyume na Yerusalemu. [26] Akaichukua hazina iliyokuwa
kwenye nyumba ya BWANA, na ile hazina iliyokuwa kwenye nyumba ya Mfalme.
Akachukua kila kitu; Pia alizichukua zile ngao za dhahabu ambazo Sulemani alikuwa
ametengeneza. [27] Mfalme Rehoboamu akatengeneza ngao za shaba mahali pake
na akazikabidhi kwa wakuu wa walinzi, ambao walilinda malango ya kuingia kwa
mfalme. [28] Na ikawa kila mfalme alipoingia kwenye nyumba ya BWANA, wale
walinzi walizibeba na baadaye walizirudisha katika chumba cha walinzi. [29] Lakini
katika mambo mengine kuhusiana na Rehoboamu, na yote yale aliyofanya, je,
hayakuandikwa kwenye kitabu cha matukio ya wafalme wa Yuda? [30] Kulikuwa na
mapigano yasiyokoma kati ya nyumba ya Rehoboamu na nyumba ya Yeroboamu.
[31] Kwa hiyo Rehoboamu akalala na mababu zake naye akazikwa pamoja nao katika
mji wa Daudi Jina la mama yake alikuwa Naama Mwamori. Abiya mwanawe akawa
mfalme mahali pake

# 15

[1] Katika mwaka wa kumi na tano wa mfame Yeroboamu mwana wa Nebati, Abiya
alianza kutawala juu yaYuda. [2] Alitawala kwa miaka mitata kule Yerusalemu. Jina
la mama yake allikuwa Maaka. Alikuwa binti wa Absalomu. [3] Naye alitembea
katika dhambi zote ambazo baba yake alizifanya kabla yake; moyo wake haukuwa
mkalifu kwa BWANA, Mungu wake kama moyo wa Daudi, babu yake ulivyokuwa.
[4] Hata hivyo, kwa ajili ya Daudi, BWANA, Mungu wake alimpa taa Yerusalemu kwa
kumwinua mwanae baada yake ili kuiimarisha Yerusalemu. [5] Mungu alifanya haya

kwa sababu Daudi alifanya yaliyo mema machoni pake; wakati wote wa uhai wake,
hakugeuka wala hakukosa katika yote aliyomwamuru, isipokuwa tu swala la Uria
Mhiti. 6 Sasa kulikuwa na vita kati ya Rehoboamu na Jeroboamu katika siku zote za
maisha ya Abiya. 7 Kwa mambo mengine ya Abiya, yote aliyofanya, je, hayajaandikwa
katika kitabu cha matukio ya wafalme wa Yuda? Sasa kulikuwa na vita kati ya Abiya
na Yeroboamu. 8 Abiya akalala na mababu zake, nao wakamzika katika mji wa Daudi.
Asa mwanae akawa mfalme mahali pake. 9 Katika mwaka wa ishirini wa Yeroboamu
mfalme wa Israeli, Asa akaanza kutawala Yuda. 10 Alitawala kwa miaka arobaini
na moja kule Yerusalemu. Bibi yake alikuwa Maaka, binti wa Absalomu. 11 Asa
akafanya yaliyo mema machono mwa BWANA, kama alivyofanya Daudi, babu yake.
12 Yeye aliwafukuza kutoka katika nchi wale makahaba wa kipagani na akaziondoa
sanamu zote ambazo babu zake walikuwa wametengeneza. 13 Pia alimwondoa bibi
yake asiwe Malkia, kwa sababu alikuwa amefanya sanamu ya kuchukiza kwa Ashera.
Asa aliikata sanamu ya kuchukiza na kuiteketeza katika Bonde la Kidroni. 14 Lakini
pale mahali pa juu hapakuchukuliwa. Hata hivyo. Moyo wa Asa ulikuwa mkamilifu
mbele ya BWANA katika siku zake zote. 15 Alivirerjesha katika nyumba ya BWANA
vitu vile vilivyokuwa vimetengwa kwa ajili ya BWANA, na vile vitu vyake vilivyokuwa
vimetengezwa kwa fedha, na dhahabu na vyombo. 16 Basi kulikuwa na vita kati
ya Asa na Baasha mfalme wa Israeli, kwa miaka yao yote. 17 Baasha mfalme wa
Israeli, akaivamia na kuijenga Rama, kiasi kwamba hakumruhusu yeyote kuondoka
au kuingia katika nchi ya Asa mfalme wa Yuda. 18 Kisha Asa akazichukua zile fedha
na dhahabu zilizokuwa zimebaki kwenye hazina kwenye nyumba ya BWANA, na
katika hazina ya ikulu ya mfalme. Akaziweka katika mikono ya watumishi wake na
kuzituma kwa Beni Hadadi mwana wa Tabrimoni mwana wa Hezioni, mfalme wa
Shamu ambaye alikuwa akishi Dameski. Akamwambia, 19 "Naomba tufanye patano
kati yangu na wewe, kama ilivyokuwa kati ya baba yangu na baba yako. Tazama,
Nimekutumia zawadi ya fedha na dhahabu. Ili uvunje agano lako na Baasha mfalme
wa Israeli, ili kwamba aniache." 20 Beni Hadadi akamsikiliza mfalme Asa na kutuma
wakuu wa majeshi yake, nao wakaishambulia miji ya Israeli. Wakaishambulia Ijoni,
Dani, Abeliya Bethi Maaka, na Kinerothi yote, pamoja na nchi yote ya Naftali. 21 Ikawa
Baasha aliposikia haya, akaacha kuijenga Rama akarudi Tirza. 22 Kisha mfalme
Asa akaitangazia Yuda yote. Hakuna aliyeachwa. Wakayabeba mawe na miti ya
Rama ambayo Baasha alikuwa akijengea mji. Kisha mfalme Asa akavitumia hivyo
vitu kuijenga Geba ya Benjamini na Mispa. 23 Mambo mengine yanyohusu utawala
wa Asa, uwezo wake wote, yote aliyofanya, na miji aliyoijenga, je, hayakuandikwa
katika kitabu cha matukio ya wafalme wa Yuda? Lakini wakati wa uzee wake alipata
ugonjwa wa miguu. 24 Kisha Asa akalala na mababu zake na akazikwa pamoja nao
katika mji wa Daudi baba yake. Yehoshafati mwanae akawa mfalme mahali pake.
25 Nadabu mwana wa Yerobiamu alianza kutawala huko Israeli wakati wa mwaka
wa pili wa Asa mfalme wa Yuda; Aliitawala Israeli kwa miaka miwili. 26 Akafanya
yaliyo maovu mbele y a macho ya BWANA naye akatembea katika njia ya baba yake,
na katika dhambi yake, aliisababisha Israeli kufanya dhambi. 27 Baasha mwana wa
Ahiya, wa familia ya Isakari, akafanya hila dhidi ya Nadabu; Baasha akamwua huko
Gibethoni, ambao ulikuwa mji wa Wafilisti, kwa kuwa Nadabu na Israeli walikuwa
wakiuhusuru Gibethoni. 28 Katika mwaka wa tatu wa Asa mfalme wa Yuda, Baasha
alimwua Nadabu naye akawa mfalme mahali pake. 29 Mara tu baad ya kuwa mfalme,
Baasha aliwaua watu wote wa familia ya Yeroboamu. Hakumwacha hata mmoja wa
uzao wa Yeroboamu awe hai; Kwa njia hii akawa ameuharibu ukoo wote wa kifalme,
kama vile BWANA alivyokuwa amesema kupitia mtumishi wake Ahiya Mshilo, 30 kwa
sababu ya dhambi za Yeroboamu ambazo alifanya na akaisababishia Israeli kufanya

dhambi, kwa kuwa alimkasirisha BWANA, Mungu wa Israeli. 31 Mambo mengine
yanayomhusu Nadabu, na yote aliyofanya, je, hayakuandikwa katika kitabu cha
matukio ya wafalme wa Israeli? 32 Kisha kulikuwa na vita kati ya Asa na Baasha
mfalme wa Israeli katika siku zao zote. 33 Katika mwaka wa tatu wa Asa mfalme
wa Yuda, Baasha mwana wa Ahiya alianza kuitawala Israeli yote huko Tirza naye
alitawala kwa miaka ishirini na nne. 34 Naye akafanya yaliyo mabaya katika macho
ya BWANA na akatembea katika njia ya Yeroboamu na katika dhambi yake ambayo
kwa hiyo aliifanya Israeli kufanya dhambi.

# 16

1 Neno la BWANA lilimjia Yehu mwana wa Hanani kinyume cha Baasha, likisema,
2 Ingawa Nilikuinua kutoka kwenye mavumbi na kukufanya kuwa kiongozi wa watu
wangu Israeli, Lakini umetembea katika njia za Yeroboamu na umewafanya watu
wangu Israeli kufanya dhambi, ili kunikasirisha dhidi ya dhambi zao. 3 Tazama,
Nitamfagia kabisa Baasha na familia yake na nitaifanya familia yako kama familia
ya Yeroboamu mwana wa Nebati. 4 Mbwa watamla yeyote ambaye anatoka kwa
Baasha wanaofia mjini, na ndege wa angani watamla yeyote anayaefia shambani."
5 Lakini kwa mambo mengine yanayohusiana na Baasha, aliyofanya, na uwezo wake,
je, hayakuandikwa katika kitabu cha matukio ya wafalme wa Israeli? 6 Baasha akalala
na mababu zake na akazikwa Tirza, na Ela mwanae akawa mfalme mahali pake.
7 Kwa kupitia nabii Yehu mwana wa Hanani neno la BWANA likaja kinyume na
Baasha na familia yake, wote kwa sababu ya maovu yote aliyofanya machoni pa
BWANA, akamghadhabisha kwa kazi ya mikono yake, kama familia ya Yeroboamu,
na kwa sababu alikuwa ameiua familia yote ya Yeroboamu. 8 Katika mwaka wa
kumi na sita wa Asa mfalme wa Yuda, Ela mwana wa Baasha akaanza kutawala juu
ya Israeli kule Tirza; akatawala kwa miaka miwili. 9 Mtumishi wake Zimri, mkuu wa
nusu ya magari yake akatengeneza hila dhidi yake. Wakati huo Ela alikuwa Tirza,
akinywa na kulewa kwenye nyumba ya Arza, ambaye alikuwa mkuu wa watumishi
wa nyumbani huko Tirza. 10 Zimri akaiingia ndani, akamshambulia na kumwua,
katika mwaka wa ishirini na saba wa Asa mfalme wa Yuda, naye akawa mfalme
mahali pake. 11 Zimri alipoaanza kutawala, mara tu baada ya kukaa kwenye kiti
cha enzi, akawaua wanafamilia wote wa Baasha. Hakumwacha mtoto hata mmoja
wa kiume, hakuna hata wa ndugu yake wala wa rafiki zake. 12 Kwa hiyo Zimri
aliingamiza familia yote ya Baasha, kama alivyokuwa ameambiwa kwa neno la
BWANA, ambalo lilinenwa kinyume na Baasha na nabii Yehu, 13 kwa dhambi zote za
Baasha na za Ela mwanae ambazo walizifanya, ambazo kwazo waliisababisha Israeli
kufanya dhambi, kiasi c ha kumghadhabisha BWANA, Mungu wa Israeli, kuzikasilikia
sanamu zao. 14 Kwa mambo mengine yanayohusiana na Ela, yote ambayo alifanya, je
hayajaandikwa kwenye kitabu cha matukio ya wafalme wa Israeli? 15 Katika mwaka
wa ishirini na saba wa Asa mfalme wa Yuda, Zimri alitawala kwa siku saba tu kule
Tirza. Jeshi likafanya kambi kule Gibethoni, ambao ni mji wa Wafilisti. 16 Lile
jeshi lililokuwa limeweka kambi kule lilisikika lilksema, "Zimri amepanga njama
na amemwua mfalme." Kwa hiyo siku hiyo hapo kambini, Israeli yote ikamtangaza
Omri, mkuu wa jeshi, kuwa mfalme wa Israeli. 17 Omri akapanda kutoka Gibethoni na
Israeli yote pamoja naye, nao wakauhusuru Tirza. 18 Kwa hiyoZimri alipoona kuwa
mji umetekwa, akaingia kwenye ngome na akaivamia ikulu ya mfalme na kulichoma
moto jengo lote pamoja na yeye; kwa hiyo akafa kwa moto. 19 Hii ilikuwa ni kwa
sababu ya dhambi alizofanya kwa kufanya maovu mbele ya macho ya BWANA, kwa
kutembea katika njia ya Yeroboamu na katika dhambi ambazo alifanya, kiasi cha
kuifanya Israeli wafanye dhambi. 20 Pia kwa mambo mengiine yanayomhusu Zimri,

na fitina yake aliyofanya, je, hayakuandikwa kwenye kitabu cha matukio ya wafalme
wa Israeli? 21 Sasa watu wa Israeli walikuwa wamegawanyika katika makundi
mawili. Nusu ya watu walimfuata Tibni mwana wa Ginathi, wakamfanya kuwa
mfalme, na Nusu walimfufata Omri. 22 Lakini watu waliomfuata Omri walikuwa
na nguvu kuliko wale waliomfuata Tibni mwana wa Ginathi. Kwa hiyo Tibni akafa,
na Omri akawa mfalme. 23 Omri alianza kutawala juu ya Israeli katika mwaka wa
thelathini na moja wa Asa mfalme wa Yuda, naye akatawala miaka kumi na miwili.
Alitawala akiwa Tirza kwa miaka sita. 24 Akakinunua kilima cha Samaria kutoka
kwa Shemeri kwa kilo 68 za fedha. Akajenga mji juu ya mlima na ule mji akauita
Samaria, kwa sababu ya jina la Shemeri, mmiliki wa awali wa kile kilima. 25 Omri
akafanya maovu mbele ya BWANA na akafanya yaliyo maovu zaidi kuliko wale
waliokuwa kabla yake. 26 Kwa kuwa alitembea katika njia zote za Yeroboamu mwana
wa Nebati na katika dhambi zake ambazo kwa hizo aliwaongoza Waisraeli kufanya
dhambi, ili kumkasirisha BWANA, Mungu wa Israeli, ili kuwa na hasira juu ya sanamu
zao za ubatili. 27 Kwa mambo mengine yanayomhusu Omri ambayo alfanya, na
nguvu zake alizoonyesha, je, hayakuandikwa katika kitabu cha matukio ya wafalme
wa Israeli? 28 Kwa hiyo Omri akalala na mababu zake na akazikwa Samaria na
Ahabu mwanae akawa mfalme mahali pake. 29 Katika mwaka wa thelathiini na
nane wa Asa mfalme wa Yuda, Ahabu mwana wa Omri akaanza kutawala juu ya
Israeli. Ahabu mwana wa Omri akatawala Israeli kule Samaria kwa miaka ishirini
na mbili. 30 Ahabu mwana wa Omri akafanya yaliyo maovu mbele ya BWANA,
zaidi ya wote waliokuwa kabla yake. 31 Ikawa kidogo tu Ahabu ayaendee makosa
ya Yeroboamu mwana wa Nebati, kwa hiyo akamwoa Yezebeli binti wa Ethibaali,
mfalme wa Wasidoni; akaenda akamwabudu baali na akamsujudia. 32 Akamjengea
madhabahu Baali, ambayo alikuwa ameijenga kule Samaria. 33 Ahabu akatengeneza
Ashera. Ahabu akafanya maovu zaidi kumghadhabisha BWANA, Mungu wa Isareli,
akamkasirisha kuliko wafalme wote wa Israeli waliokuwa kabla yake. 34 Katika siku
zake Hieli Mbetheli aliijenga tena Yeriko. Akaijenga misingi ya mji kwa kufiwa na
Abiramu mzaliwa wake wa kwanza, naye akayajenga malango ya mji kwa kufiwa
na mwanae mdogo Segebu, na walifanya hivi kwa sababu walitii neno la BWANA,
ambalo alikuwa amelinena kwa kinywa cha Joshua mwana wa Nuni.

# 17

1 Eliyas Mtishibi, kutoka Tishibi ya Gileadi, akamwambia Ahabu, “Kama BWANA,
Mungu wa Israeli aishivyo, ambaye ninasimama, hakutakuwa na umande wala
mvua isiipokuwa kwa neno langu.” 2 Kisha nenola BWANA, likammjia Eliya,
likisema, 3 “Ondoka hapa uende mashariki; ukajifiche karibu na kijito cha Kerithi,
mashariki mwa Yorodani. 4 Nawe utakunywa maji ya kijito, na nimewaamuru
kunguru kukulisha mahali hapo.” 5 Kwa hiyo Eliya akaenda kama neno la BWANA
lilivyomwamuru. Akaenda kuishi karibu na kijito cha Kerithi, mashariki mwa
Yorodani. 6 Nao kunguru wakamletea mkate na nyama asubuhi, na mkate na
nyama jioni, naye akanywa maji ya kijito kile. 7 Lakini baada ya muda kile kijito
kikakauka kwa sababu hapakuwepo na mvua katika nchi. 8 Neno la BWANA likamjia,
likisema, 9 “Inuka, uende Sarepta, ambao ni mji wa Sidoni, na ukaishi huko. Tazama
nimemmwamuru mjane kukulisha.” 10 Kwa hiyo akainuka na akaenda Sarepta,
na alipofika kwenye lango la mji, kulikuwa na mjane akiokota kuni. Kwa hiyo
akamwita na akamwambia, “Tafadhali niletee maji kidogo kwenye jagi ninywe.”
11 Naye alipokuwa akienda kuleta maji alimwita, akamwambia, “tafadhali uniletee
na kipande cha mkate mkononi.” 12 Naye akamjibu, “Kama BWANA Mungu wako
aishivyo, sina mkate wowote, bali konzi moja ya unga katika chombo na mafuta

kidogo kwenye chupa. Tazama, ninaokota kuni mbili ili niende kupika kwa ajili
yangu na mwanangu, ili tule, na tusubiri kufa.” 13 Eliya akamwambia, “Usiogope.
Nenda ukafanye kama usemavyo. lakini nitengenezee kwanza mimi na uniletee.
Ndipo baadaye ujitenegenezee wewe na mwanao. 14 Kwa kuwa BWANA, Mungu
wa Israeli anasema 'Lile pipa la unga halitaisha, wala ile chupa ya mafuta kukoma
kutoa mafuta, mpaka siku ile BWANA atakapotuma mvua duniani.” 15 Kwa hiyo yule
mjane akafanya kama Eliya alivyomwelekeza, yeye, na Eliya, na mwanae wakala kwa
siku nyingi. 16 Lile pipa la Unga halikuisha, wala ile chupa ya mafuta haikukoma
kutoa mafuta, kama vile neno la BWANA lilivyosema, kupitia kinywa cha Eliya.
17 Baada ya hayo mambo, yule mwana wa yule mwanamke, yule mwanamke mwenye
nyumba, aliugua. Ugonjwa wake ukazidi hata akaishiwa pumzi kabisa. 18 Kwa
hiyo mama yake akamwambia Eliya, “Je, una nini nami, ewe mtu wa Mungu?
Je, umekuja kwangu ili kunikumbusha dhambi zangu na kumwua mwanangu?”
19 Naye Eliya akamjibu, “Nipe hapa mwanao.” Akambeba mtoto mikononi mwake na
akampeleka mpaka chumbani alimokuwa akikaa, akamlaza yule mtoto kitanadani
pake mwenyewe. 20 Akamlilia BWANA akisema, “BWANA Mungu wangu, kwa
nini umeleta majanga kwa mjane ambaye mimi ninakaa, kwa kumwua mwanae?”
21 Kisha Eliya akajinyosha mwenyewe juu ya mtoto mara tatu; akamlilia BWANA
akisema, “BWANA Mungu wangu, Ninakuomba, tafadhali uhai wa mtoto huyu
umrudie.” 22 BWANA akaisikiliza sauti ya Eliya; uhai wa mtoto ukamrudia, na akawa
hai. 23 Eliya akamchukua mtoto na akamtoa toka chumbani kwake akamleta kwenye
ile nyumba; akampatia mama yake yule mtoto na akasema, “Tazama, mwanao yuko
hai.” 24 Yule mwanamke akamwambia Eliya, “Sasa natambua kuwa wewe ni mtu wa
Mungu, na kwamba neno la BWANA kinywani mwako ni la kweli.”

# 18

1 Kwa hiyo baada ya siku nyingi neno la BWANA likamjia Eliya, katika mwaka
wa tatu wa ukame, likisema, “Nenda ukajionyeshe mwenyewe kwa Ahabu nami
nitainyeshea ardhi mvua.” 2 Eliya akaenda kujionyesha mwenyewe kwa Ahabu;
sasa njaa ilikuwa kali sana kule Samaria. 3 Ahabu akamwita Obadia, aliyekuwa
mkuu wa ikulu. Obadia alimheshimu sana BWANA, 4 kwa kuwa wakati Yezebeli
alipokuwa akiwaua manabii wa BWANA, Obadia alichukua manabii mia akawaficha
katika makundi ya hamsini hamsini katika pango na akawalisha kwa mikate na maji.
5 Ahabu akamwambia Obadia, “Pita katika nchi yote na katika chemichemi zote za
maji na vijito. Yamkini tunaweza kupata maji na nyasi ili tuwaokoa hawa farasi na
nyumbu, ili tusiwakose wanyama wote.” 6 Kwa hiyo wakaigawa nchi kati yao ili
wapite kati yake wakitafuta maji. Ahabu akaenda njia yake mwenyewe na Obadia
naye akaenda njia yake. 7 Wakati Obadia akiwa njiani, akakutana na Eliya pasipo
kutegemea. Obadia akamtambua na akalala kifudifudi chini. Akamwambia, “Ndiye
wewe, bwana wangu Eliya?” 8 Naye Eliya akamjibu, Ni mimi. Nenda umwambie
bwana wako, 'Tazama, Eliya yuko hapa.'” 9 Obadia akamjibu. “Nimekoseaje, kwamba
umtoe mtumishi wako katika mkono wa Ahabu ili aniue? 10 Kama BWANA Mungu
wako aishivyo, hakuna taifa wala ufalme ambapo bwana wangu hajatuma watu
kukutafuta. Kila taifa au ufalme unaposema, “Eliya hayuko hapa,' Ahabu hufanya
waape ni kweli hawajakuona. 11 Na sasa wewe unasema, 'Nenda, ukamwambie
bwana wako kwamba Eliya yuko hapa.' 12 Mara tu baada ya kukuacha Roho wa
BWANA atakuchukua na kukupeleka mahali ambapo sitapajua. Kisha nikienda na
kumwambia Ahabu, na asipokuona, ataniua. Bado, mimi, mtumishi wako, nimekuwa
nikimwabudu BWANA kutoka ujana wangu. 13 Je, haujaambiwa, bwana wangu,
nilichokifanya wakati Yezebeli alipowaua manabii wa BWANA, jinsi nilivyowaficha

wale manabii mia moja wa BWANA katika makundi ya hamsini kwenye pango na
kuwalisha kwa mikate na maji? 14 Na sasa unasema, 'Nenda umwambie bwana
wako kwamba Eliya yuko hapa,' kwa hiyo ataniua." 15 Ndipo Eliya alipomjibu,
"Kama vile BWANA wa majeshi aishivyo, ambaye mimi ninasimama, Kwa hakika
nitajionyeshakwa Ahabu leo." 16 Kwa hiyo Obadia akaenda kukutana na Ahabu,
nakumwambia kile Eliya alichokuwa amemwambia. Ndipo mfalme alipoenda
kukutana na Eliya. 17 Ahabu alipomwona Eliya, akamwambia, "Je, ni wewe? Wewe
mtabishaji wa Israeli!" 18 Eliya akamwambia, "Mimi sijaitabisha Israeli, Lakiini
wewe na familia ya baba yako ndio watabishaji kwa kuziacha amri za BWANA na
kufuata sanamu za Baali. 19 Kwa hiyo sasa, Tuma neno na unikusanyie Israeli yote
katika mlima Kameli, pamoja na manabii 450 wa Baali na wale manabii 400 wa
Ashera wanaokula kwenye meza ya Yezebeli." 20 Kwa hiyo Ahabu akatuma neno
kwa watu wote wa Israeli na akawakusanya manabii wote kwenye mlima Kameli.
21 Eliya akaja karibu na watu wote akasema, "Mtaendelea kubadilisha mawazo yenu
mpaka lini? Kama BWANA ni Mungu, mfuateni yeye, Lakini kama Baali ni Mungu,
basi mfuateni yeye," Lakini watu hawakumjibu neno. 22 Kisha Eliya akawaambia
wale watu, "Mimi, pekee yangu, ndiye niliyebaki kuwa nabii wa BWANA, lakini
manabii wa Baali wako 450. 23 Hebu tutoleeni ng'ombe wawili. Nao wajichagulie
ng'ombe mmoja na wamchinje na kumkatakata katika vipnde, na wamweke kwenye
kuni, na wasitie moto chini yake. Nami nitamwandaa yule wa pili na kumweke
juu ya kuni nami sitatia moto chini yake. 24 Kisha mtaliita jina la mungu wenu,
nami nitaliita jina la BWANA, na Mungu atakayejibu kwa moto, huyo ndiye Mungu."
Watu wote wakajibu na kusema, "Hilo ni jambo jema." 25 Kwa Eliya akawaambia
manabii wa Baali, "Chagueni ng'ombe mmoja kwa ajili yenu na mwe wa kwanza
kumwamdaa, kwa kuwa ninyi ni wengi, Kisha liiteni jina la mungu wenu, lakini
msiwashe moto." 26 Nao wakamchukua yule ng'ombe waliokuwa wamepewa na
wakamwandaa, na ndipo walipoliita jina la Baali kuanzia asubuhi hadi adhuhuri,
wakisema, "Baali, tusikie." Lakini hapakuwepo na Sauti, na wala hakuna aliyejibu.
Wakachezacheza kuizunguka madhabahu waliyotengeneza. 27 Ilipofika adhuhuri
Eliya akawakejeli akisema, "Mwiteni kwa nguvu! Huyo ni mungu! labda anawaza
kitu, au amepumzika, au yuko safarini, au pengine amelala sharti aamshwe." 28 Kwa
hiyo wakamwita kwa nguvu, wakajikatakata kama kawaida yao ilivyokuwa, kwa
upanga na nyembe, mpaka damu ikawachuruzika. 29 Ikawa wakati wa adhuhuri
ulipopita, na bado walikuwa wakiendelea kutabiri mpaka wakati wa jioni wa kutoa
dhabihu, lakini hapakuwepo na sauti wala mtu wa kuwajibu; wala hapakuwepo
na yeyote wa kujibu wala wa kuangalia. 30 Kisha Eliya akawaambia watu wote,
"Nisogeleeni," na watu wote wakamsogelea. Naye akatengeneza ile madhabahu ya
BWANA ambayo ilikuwa imeharibika. 31 Eliya akachukua mawe kumi na mawili, kila
jiwe moja liliwakilisha kabila moja la wana wa Yakobo - ni kupitia Yakobo kwamba
neno la BWANA lilikuja, likisema, "Jina lako litakuwa Israel." 32 Kwa kutumia hayo
mawe aliijenga ile madhabahu kwa jina la BWANA na akachimba mfereji kuizunguka
ile madhabahu kubwa kiasi cha kubeba lita kumi na tano za maji. 33 Kisha akaweka
kuni kwa ajili ya moto na akamkatakata yule ng'ombe katika vipande vipande na
akaweka vile vipande juu ya kuni. Na akasema, "Vijazeni maji hivyo vyombo na
yamwageni kwenye hiyo sadaka ya kueketezwa na juu ya hizo kuni." 34 Akasema
tena fanyeni hivyo mara ya pili," nao wakafanya kwa mara ya pili. kisha akasema,
"Fanyeni mara ya tatu," nao wakafanya kwa mara ya tatu. 35 Maji yakaizunguka ile
madhabahu na kuujaza ule mfereji. 36 Ikawa wakati wa kutoa dhabihu ya jioni,
nabii Eliya akasogea na akasema, "BWANA, Mungu wa Abrahamu, na wa Isaka,
na wa Israeli, na ijulikane leo kwamba wewe ndiye Mungu wa Israeli, na kwamba

mimi ni mtumishi wako, na kwamba nimeyafanya mambo haya yote kwa jina lako.
37 Nisikie, BWANA, nisike, ili hawa watu wajue kuwa wewe, BWANA, ndiye Mungu, na
kwamba umeirudisha mioyo yao kwako tena." 38 Ndipo moto wa BWANA ukashuka
ukairamba ile sadaka, pamoja na zile kuni, mawe na mavumbi, na kuyaramba
yale maji yaliyokuwa kwenye ule mfereji. 39 watu wote walipoona haya, wakalala
kifudifudi chini wakasema, "BWANA, ndiye Mungu! BWANA ndiye Mungu! 40 Kwa
hiyo Eliya akawaambia, "Wakamateni manabii wa Baali. Msimwache hata mmoja
wao atoroke." Kwa hiyo wakawakamata, na Eliya akawaleta manabii wa Baali chini
kwenye kijito cha Kishoni na akawaua huko. 41 Eliya akamwambia Ahabu, "Inuka,
ule na kunywa, kwa kuwa kuna sauti ya mvua kubwa." 42 Kwa hiyo Ahabu akaenda
akala na knywa. Kisha Eliya akaenda juu ya mlima Kameli, akasudu chini na akaweka
uso wake katikati ya magoti. 43 Akamwambia mtumishi wake, "Nenda sasa, utazame
upande wa bahari." mtumishi wake akaenda na akasema, "Hakuna kitu," Eliya
akamwambia, "Nenda tena, mpaka mara saba." 44 Ile mara ya saba mtumishi wake
akasema, "Tazama, kuna wingu linapanda kutoka baharini, ni dogo kama mkono wa
mtu." Eliya akamjibu, Nenda ukamwambie Ahabu, 'Andaa gari lako na ushuke kabla
mvua haijakuzuia.'" 45 Ikatokea baada ya muda mfupi mbingu zikawa nyeusi kwa
mawingu na upepo, na kulikuwa na mvua kubwa. Ahabu akapanda gari akaenda
zake Yezreeli, 46 lakini mkono wa BWANA ulikuwa juu ya Eliya. Akalikaza vazi lake
kwa mshipi wake na akakimbia mbele ya Ahabu kwenye lango la Yezreeli.

# 19

1 Ahabu akamwambia Yezebeli mambo yote ambayo Eliya amefanya na jinsi
alivyowaua manabii wote kwa upanga. 2 Ndipo Yezebeli alipotuma mjumbe kwa
Eliya, akisema, "miungu wanifanye hivyo na mimi, na zaidi yake, kama kesho muda
kama huu sitayafanya maisha yako kuwa kama mmoja wa hao manabii waliokufa."
3 Eliya aliposikia hayo, akaiinuka na akakimbia kwa ajili ya kuokoa maisha yake
akaja mpaka Beerisheba, ambao ni mji wa Yuda, na akamwacha mtumishi wake
huko. 4 Lakini yeye mwenyewe akaenda mwendo wa siku moja huko jangwani,
akaja akakaa chini ya mti wa mretemu. Akajiombea mwenyewe kufa, akasema,
"Sasa yatosha, BWANA, ichukue roho yangu, kwa kuwa mimi si mzuri kuliko mababu
zangu waliokufa." 5 Kwa hiyo akalala chini ya mretemu. Ghafula malaika akamgusa
na akamwambia, "Inuka ule." 6 Eliya akatazama, karibu na kichwa chake kulikuwa
na mkate uliokuwa umeokwa kwa mkaa na gudulia la maji. Kwa hiyo akala na
kunywa na kulala tena. 7 Malaika wa BWANA akaja tena mara ya pili akamgusa
na kumwambia, "Inuka ule, kwa sababu safari bado ndefu kwako." 8 Kwa hiyo
akainuka na kula na kunywa, naye akasafiri kwa nguvu ya chakula hicho kwa siku
arobaini mchana na usiku hata akafika Horebu, mlima wa Mungu. 9 Akaingia kwenye
pango akakaa humo. Kisha neno la BWANA likamjia likimwambia, "Unafanya
nini hapa, Eliya?" 10 Eliya akajibu, "Nimeona wivu mwingi kwa BWANA, Mungu
wa majeshi, kwa kuwa watu wa Israeli wameliacha agano lako, wameziharibu
madhabahu zako, na wamewaua manabii wako kwa upanga. Sasa ni mimi, pekee
yangu, nimebaki na wanataka kuichukua roho yangu. 11 BWANA akamwambia,
"Nenda nje ukasimame kwenye mlima mbele yangu." Kisha BWANA akapita, na
upepo mkali ukaupiga mlima ukavunja miamba katika vipande vipande mbele ya
BWANA, lakini BWANA hakuwemo kwenye huo mlima. Kisha baada ya upepo,
tetemeko lakaja, lakini BWANA hakuwemo kwenye hilo tetemeko. 12 Kisha baada
ya tetemeko, moto ukaja, lakini BWANA hakuwemo kwenye moto. Ndipo baada
ya moto, sauti ya upole ikaja. 13 Naye Eliya alipoisikia sauti, akafunika uso wake
kwa vazi lake, akatoka nje, akasimama kwenye lango la hilo pango. Na sauti ikaja

kwake ikisema, “unafanya nini hapa?, 14 Eliya akajibu, “nimeona wivu sana kwa
ajili ya BWANA, Muungu wa majeshi, kwa kuwa watu wa Israeli wameliacha agano
lako, wameziharibu madhabahu zako, na wamewaua manabii kwa upanga. Sasa,
ni mimi pekee yangu, nimebaki na wanajaribu kuichukua roho yangu.” 15 Kisha
BWANA akamwambia, “Nenda, rudi kwa njia yako kwenye jangwa la Dameski, na
utakapofika utamtia mafuta Hazaeli awe Mfalme wa Shamu, 16 na utamtia mafuta
Yehu mwana wa Nimshi kuwa mfalme wa Israeli, na utamtia mafuta Elisha mwana
wa Shafeti wa Abeli Mehola kuwa nabii mahali pako. 17 Itakuwa hivi Yehu atamwua
kila mmoja atakayejaribu kutoroka upanga wa Hazaeli, na kwamba Elisha atamwua
kila atakayejaribu kukwepa upanga wa Yehu. 18 Lakini nitawaacha watu elfu saba
katika Israeli kwa ajili yangu, ambao magoti yao hayajawahi kupigwa kwa Baali,
na ambao midomo yao haijambusu.” 19 Kwa hiyo Eliya akaondoka mahali pale
na akamkuta Elisha mwana wa Shafati, akilima na jozi za makisai kumi na mbili
mbele yake, na yeye mwenyewe alikuwa akilima na ile jozi ya kumi na mbili. Eliya
akaenda mpaka kwa Elisha akamtupia vazi lake juu yake. 20 Elisha naye akawaacha
wale makisai akamkimbilia Eliya; akamwambia, “Tafadhali naomba nikambusu baba
yangu na mama yangu kisha nitakufuata.” Naye Eliya akamwambia, “Rudi, lakini
fikiria juu ya kile nilichokufanyia.” 21 Kwa hiyo Elisha akarudi toka kwa Eliya na
akachukua ile jozi ya makisai, akawaua wale wanyama, na akapika ile nyama kwa
kuni za ile nira. Kisha akawapa watu wakala. Kisha akaamka, akamfuata Eliya
akamtumikia.

# 20

1 Beni Hadadi mfalme wa Shamu akakusanya jeshi lake lote pamoja. Kulikuwa na
wafalme thelathini na mbili wasaidizi pamoja naye, na magari na farasi. Akapanda,
akaihusuru Samaria na kupigana nayo. 2 Akatuma wajumbe katika mji kwa Ahabu
mfalme wa Israeli, akamwambia, “Beni Hadadi anasema hivi: 3 Fedha zako na
dhahabu zako ni zangu. Pia wake zako na watoto, wale wazuri, sasa ni wangu.”
4 Mfalme wa Israeli akajibu akasema, “Na iwe kama unavyosema, bwana wangu,
mfalme. Mimi pamoja na vile nilivyo navyo ni mali yako.” 5 Wale wajumbe
wakaja tena wakasema, “Beni Hadadi anasema hivi, 'Nilituma neno kwako nikisema
kwamba lazima ukabidhi kwangu fedha zako, dhahabu zako, wake zako na watoto
wako. 6 Lakini kesho nitatuma watumishi wangu kwako wakati kama huu, nao
wataichunguza nyumba yako na nyumba za watumishi wako. Nao watatia mikononi
mwao na kukichukua kila wakipendacho machoni mwao.'” 7 Ndipo mfalme wa
Israeli akawaita wazee wote wa nchi pamoja akawaambia, ''Hebu angalieni jinsi huyu
mtu anavyotafuta matatizo. Amenitumia ujumbe kwamba anataka kuchukua wake
zangu, watoto wangu, fedha na dhahabu zangu, nami sijamkatalia.” 8 Wazee wote
na watu wote wakamwambia Ahabu, “Usimsikilize wala kukubaliana na matakwa
yake.” 9 Ahabu akawaambia wajumbe wa Beni Hadadi, “Mwambieni bwana wangu
mfalme kwamba, 'Ninakubaliana na kila kitu ambacho kwanza uliwatuma watumishi
wako kufanya kwangu, lakini sikubaliani na matakwa yako haya ya pili.'” Wale
watumishi wa Beni Hadadi wakaondoka wakampelekea mrejesho Beni Hadadi.
10 Naye Beni Hadadi akatuma tena majibu yake kwa Ahabu, akaisema, “basi miungu
inifanyie hivyo na zaidi, kama hata mavumbi ya Samaria yatawatosheleza watu
watu wote wanaonifuata kuchukua kila mmoja angalau konzi mkononi mwake.”
11 Naye mfalme wa Israeli akamjibu akisema, “Mwabieni Beni Hadadi, 'Hakuna
abebaye silaha yake, atakayejivuna kama wakati wa kuishusha.”' 12 Beni Hadadi
aliusikia ujumbe huu wakati alipokuwa akinywa, yeye na wafalme walikuwa pamoja
naye waliokuwa kwenye mahema yao. Beni Hadadi akayaamuru majaeshi yake,
“Jipangeni katika sehemu zenu kwa ajili ya vita.” Kwa hiyo wakajiandaa kivita

ili kuuvamia mji. 13 Tazama, nabii akaja kwa Ahabu mfalme wa Israeli akasema,
“BWANA asema, 'Je umeliona hili jeshi kubwa? Tazama, nitaliweka katika mkono
wako leo, nawe utatambua kuwa mimi ni BWANA.'” 14 Naye Ahabu akajibu, ''kwa
nani? BWANA akamjibu akasema, “kwa kuwatumia viijana wanaotumikia maliwali
wa wilaya.” kisha Ahabu akasema, “Ni nani atakayepewa hiyo vita?' BWANA
akamwambia, “wewe.” 15 Ndipo Ahabu alipowataarifu wale vijna wanaowatumikia
maliwali wa wilaya. Idadi yao ilikuwa 232. Baada yao aliwahesabu wanajeshi
wote, jeshi lote la Israeli; idadi yao ilikuwa elfu saba. 16 Nao wakatoka wakati wa
adhuhuri. Naye Beni Hadadi alikuwa akinywa na kulewa hemani mwake, yeye
na wale wafalme wadogo thelathini na mbili waliokuwa wakimsaidia. 17 Wale
maakida vijana waliokuwa wakiwasaidia maliwali wa wilaya walitangulia kwanza.
Kisha Beni Hadadi alitaarifiwa na wanaskauti aliokuwa amewatuma kwamaba,
“kuna watu wanakuja kutoka Samaria.” 18 Beni Hadadi akasema, “wawe wamekuja
kwa amani au kwa vita, wakamteni wakiwa hai.” 19 Kwa hiyo wale vijvana
wanaowatumikia maliwali wa wilaya wakaenda mjini na jeshi likawafuata kwa
nyuma. 20 Kila mmoja akaua adui wake na wale washami wakakimbia. Israeli
ikawashinda. Beni Hadadi mfalme wa Shamu akatoroka kwa farasi pamoja na
wapanda farasi. 21 Kisha mfalme wa Israeli akaenda akawashambulia farasi na
magari, na kuwaua washami kwa mauaji makubwa. 22 Yule nabii akaja kwa mfalme
wa Israeli akamwambia, “Nenda, ukajiimarishe mwenyewe, uelewa na kupanga kile
unachofanya, kwa sababu mwakani mfalme wa Shamu atapanda dhidi yako tena.”
23 Wale watumishi wa mfalme wa Shamu wakamwambia, “Mungu wao ni mungu
wa milimani. Hiyo ndiyo sababu walikuwa na nguvu kuliko tulivyokuwa. Lakini
sasa hebu tupigane nao katika nchi tambarare, na kwa hakika tutakuwa na nguvu
kuliko wao. 24 Na ufanye hivi: waondoe wafalme; mwondoe kila mmoja mahali pake
ukaweke majemedari mahali pao. 25 Kisha ujihesabie jeshi kama lile jeshi ulilopoteza,
farasi kwa farasi na gari kwa gari, nasi tutapigana nao katika nchi tambarare. Kwa
hakika tutakuwa na nguvu kuliko walivyo.” Kwa hiyo Beni Hadadi akausikiliza
ushauri huo naye akafanya kama alivyoshauriwa. 26 Baada ya mwanzo wa mwaka
mpya, Beni Hadadi akawahesabu Washami na akapanda Afeki kupigana na Israeli.
27 Watu wa Israeli walikuwa wamehesabiwa na walikuwa wamejipanga kupigana
nao. Watu wa Israeli wakafanya kambi mbele yao kama makundi mawili madogo
ya mbuzi, lakini Washami wakaujaza upande wa nchi. 28 Ndipo mtu wa Mungu
akaja karibu akaongea mfalme wa Israeli akamwambia, “BWANA anasema: 'Kwa
kuwa Washami wamesema kuwa BWANA ni mungu wa milima, na wala si mungu
wa mabondeni, nitaliweka hili jeshi kubwa mkononi mwako, nawe utajua kuwa mimi
ni BWANA.'” 29 Kwa hiyo majeshi yakaweka kambi yakikabiliana kwa muda wa siku
saba. Kisha siku ya saba vita vikaanza. Watu wa Israeli wakawaua Washami 100,
000 wanajeshi wa ardhini kwa siku moja. 30 Waliobaki wakakimbilia Afeki, mjini,
na ule ukuta ukaanguka juu ya watu ishiriinina saba elfu waliobaki. Naye Beni
Hadadi akakimbilia mjini. akaingia kwenye chumba cha ndani. 31 Wale watumishi
wa Beni Hadadi wakamwambia, “Tazama sasa, tumesikia kwamba wale wafalme
wa nyumba ya Israeli ni wenye rehema. Tafadhali hebu tuvaeni magaunia viunoni
mwetu na kamba vichwani mwetu, na twendeni kwa mfalme wa Israeli. Labda
atakuokoa roho yako.” 32 Kwa hiyo wakavaa magunia viunoni mwao na kujifunga
kamba vichwani mwao na kisha wakaenda kwa mfalme wa Israeli wakamwambia,
“Mtumishi wako Beni Hadadi, anasema, 'tafadhali niachie uhai wangu.” Ahabu
akawaambia, “Je, bado yuko hai? Yeye ni ndugu yangu.” 33 Sasa wale watu
walikuwa wakisikiliza ishara yeyote kutoka kwa Ahabu, kwa hiyo wakamjibu haraka,
“Ndiyo ndugu yako Beni Hadadi bado yuko hai.” Ahabu akawaambia, “Nendeni

mkamlete.” Ndipo Beni Hadadi alipokuja kwake, na Ahabu akamwacha aje kwenye
gari lake. 34 Beni Hadadi akamwambia Ahabu, “Nitakurudishia miji yako ambayo
baba yangu alichukua toka kwa baba yako, na unaweza kutengeneza masoko kwa
ajili yako Dameski, kama baba yangu alivyofanya kule Samaria.” Ahabu akajibu,
“Nitakuacha uende kwa agano hili.” Kwa hiyo Ahabu akafanya agano naye kisha
akamwacha aende. 35 Mtu mmoja, mmoja wana wa wana wa manabii, akamwambia
mmoja wa wale manabii wenzake kwa neno la BWANA, “Tafadhali nipige.” Lakini
yule mtu akakataa kumpiga. 36 Kisha yule nabii akamwambia nabii mwenzake,
“ Kwa sababu umekataa kutii sauti ya BWANA, mara tu utakaponiacha, simba
atakuua.” na mara tu baad ya yule mtu kumwacha, simba akamkuta na kumwua.
37 Kisha yule nabii akamkuta mtu mwingine akamwambia, “Tafadhali nipige.”Yule
mtu akampiga na kumwumiza. 38 Kisha yule nabii akaondoka akaenda kumsubiri
yule mfalme barabarani; naye alikuwa amejibadilisha kwa kilemba machoni pake.
39 Ikawa mfalme alipokuwa akipita, Yule nabii akamwita mfalme na kumwambia,
“Mtumishi wako aliienda katikati ya pigano, na askari akasimama akamleta adui
kwangu akasema, 'Mwangalie mtu huyu. Na ikiwa kwa vyovyote atatoroka, basi
maisha yako yatatolewa kwa ajili ya maisha yake vinginevyo utalipa kilo thelathini
za fedha. 40 Lakini kwa kuwa mtumishi wako alikuwa na mambo mengi akienda
huku na kule, yule askari adui akatoroka.” Basi mfalme wa Israeli akamwambia,
Hivyo ndivyo itakavyokuwa hukukmu yako - umejihukumu mwenyewe.” 41 Ndipo
yule nabii alipoondoa haraka kile kilemba machoni pake, na mfalme wa Israeli
alipotambua kuwa huyo alikuwa mmoja wa manabii. 42 Yule nabii akamwambia
mfalme, “BWANA anasema, 'Kwa sababu umemwachia aende mtu yule niliyekuwa
nimemhukumu kifo, maisha yako yatachukua nafasi ya maisha yake.'” 43 Kwa hiyo
mfalme wa Israeli akaenda nyumbani kwake akiwa na moyo mzito na mwenye
hasira, akafika Samaria.

# 21

1 Basi ikawa baada ya hayo, Nabothi Myezreeli alikuwa na shamba la mizabibu
kule Yezreeli, karibu na ikulu ya Ahabu, mfalme wa Samaria. 2 Ahabu akamwambia
Nabothi, akisema, “Nipe shamba lako, ili nilifanye kuwa bustani ya mboga, kwa
sababu iko karibu na nyumba yangu. Badala yake nitakupa shamba zuri la mizabibu,
au, kama ukipenda nitakulipa thamani yake kwa fedha.” 3 Nabothi akamjibu Ahabu,
“BWANA na alizuie hilo nisije nikatoa urithi wa mababu zangu kwako.” 4 Ahabu
akaingia kwenye ikulu yake akiwa mchovu na mwenye hasira kwa sababu ya jibu
ambalo Nabothi Myezreeli alimpa aliposema, “Sitakupa urithi wa mababu zangu.”
Akalala kitandani kwake, akiwa amegeuza uso wake upande ule, na akagoma kula
chakula chochote. 5 Yezebeli mke wake akaiingia kwake, akamwambia “Kwa nini
moyo wako una huzuni, kiasi kwamba hutaki kula?” 6 Naye akamjibu,” Niliongea
na Nabothi Myezreeli nikamwambia, 'Nipe shamba lako nami nitakupa pesa, au
kama inakupendeza, nitakupa shamba jingine ili liwe lako.' Naye akanijibu, 'Sitakupa
shamba langu.'” 7 Naye Yezebeli mkewe akamjibu, “Je, wewe si mtawala wa ufalme
wa Israeli? Inuka ule; na moyo wako uwe na amani. Nitalichukua hilo shamba
la mizabibu la Nabothi Myezreeli kwa ajili yako. 8 Kwa hiyo Yezebeli akaandika
barua kwa jina la Ahabu, akaitia muhuri wake, akazituma kwa wazee na kwa
watu tajiri alioketi nao kwenye vikao, na ambao pia waliishi karibu na Nabothi.
9 Katika ile barua aliyoandika, ilisema hivi, “Pigeni mbiu ya kufunga mkamkalishe
Nabothi juu mbele ya watu. 10 Pia mwaweke watu wawili wasiokuwa waaminifu
pamoja naye na wale watu watoe ushahidi kinyume naye, waseme, 'Ulimlaani Mungu
na mfalme.”Halafu mchukueni nje mkampige kwa mawe mpaka afe. 11 Kwa hiyo

watu wa mji wake, wazee na watu tajiri waishio kwenye huo mji, wakafanya kama
Yezebeli alivyowaeleza, kama ilivyoandikwa kwenye zile baraua ambazo alikuwa
amewatumia. 12 Wakapiga mbiu ya kufunga wakamkalisha Nabothi juu mbele ya
watu. 13 Na wale watu wawili wasiokuwa waaminifu wakaja wakakaa mbele ya
Nabothi; nao wakatoa ushuhuda wao dhidi ya Nabothi kuwa amemlaani Mungu
na mfalme." Kisha wakamchukua nje ya mji wakampiga kwa mawe mpaka akafa.
14 Kisha wazee wakatuma neno kwa Yezebeli, wakisema, "Nabothi ameshapigwa
mawe na amekufa." 15 Naye Yezebeli aliposikia kuwa Nabothi ameshapigwa mawe
na alikuwa amekufa, akamwabia Ahabu, "Inuka na ukamiliki shamba la mizabibu
la Nabothi Myezreeli, ambalo alikataa kukuuzia, kwa sababu Nabothi hayuko hai,
bali amekufa." 16 Ahabu aliposikia kuwa Nabothi amekufa, akainuka ili aende
kwenye lile shamba la mizabibu la Nabothi Myezreeli na kulimiliki. 17 Ndipo neno
la BWANA likamjia Eliya Mtishibi, likisema, 18 "Inuka uende ukakutane na Ahabu
mfalme wa Israeli, ambaye anaishi Samaria. Yumo kwenye shamba la Nabothi,
ambako ameenda kuchukua umiliki wa shamba hilo. 19 Ukaongee naye umwambie
kwamba BWANA anasema, 'Je, umeua na kujimilikisha?' na utamwambia kwamba
BWANA anasema, 'Mahali pale ambapo mbwa wameramba damu ya Nabothi, ndipo
mbwa watakaporamba damu yako, ndiyo, damu yako.'" 20 Ahabu akamwambia Eliya,
"Je, umenipatia, adui yangu?" Eliya akamjibu, "Nimekupata wewe kwa sababu,
umejiuza mwenyewe kufanya yaliyo maovu mbele ya macho ya BWANA. 21 BWANA
anakwambia hivi: 'Tazama, Nitaleta janga kwako na litakuangamiza kabisa na
kufutilia mbali kila mtoto mume na mtumwa na mtu huru katika Israeli. 22 Nitaifanya
familia yako kama familia ya Yeroboamu mwana wa Nebati, na kama familia ya
Baasha mwana wa Ahiya, kwa sababu umenighadhabisha na umewasababisha Israeli
kufanya dhambi. 23 Pia BWANA ameongea kuhusu Yezebeli, amesema, "mbwa
watamla Yezebeli pembeni mwa ukuta wa Yezreeli.' 24 Yeyote ambaye ni mtu wa
familia ya Ahabu ambaye atafia mjini - mbwa watamla. Na yeyote ambaye atafia
shambani - ataliwa na ndege wa angani." 25 Hapakuwepo na mtu kama Ahabu,
ambaye alijiuza mwenyewe kufanya maovu mbele ya macho ya BWANA, ambaye mke
wake Yezebeli alimchochea kufanya dhambi. 26 Ahabu alifanya matendo yachukizayo
kwa ajili ya sanamu alizofanya, kama vile yale yote ambayo Waamori walifanya,
BWANA akawafukuza mbele ya watu wa Israeli. 27 Ahabu aliposikis maneno haya,
Akachana mavazi yake na akavaa magunia kwenye mwili wake na akfaunga, na
akalala kwenye magunia na akahuzunika sana. 28 Kisha neno la BWANA likamjia
Eliya Mtishibi likisema, 29 "Je, unamwona jinsi Ahabu anavyojinyenyekeza mbele
yangu? Kwa sababu anajinyeyenyekeza mwenyewe mbele yangu, Sitaleta lile janga
katika siku zake; Ni katika siku za mwanae, nitakpolileta hilo janga katika familia
yake."

## 22

1 Miaka mitatu ilipita bila kuwepo na vita kati ya Washami na Wisraeli. 2 Ikawa
katika mwaka wa tatu, Yehoshafati mfalme wa Israeli akashuka kwa mfalme wa
Isreli. 3 Mfalme wa Israeli alikuwa amewaambia watumishi wake, "Je, mnajua kuwa
Ramothi Gileadi ni yetu, ila hatufanyi chochote kuitwaa kutoka kwenye mkono wa
mfalme wa Shamu?" 4 Kwa hiyo akamwambia Yehoshafati, "Je, utakwenda na mimi
katika vita huko Ramothi Gileadi?" Yehoshafati akamjibu mfalme wa Israeli, "Mimi ni
kama wewe, watu wangu ni kama watu wako, na farasi wangu ni kama farasi wako."
5 Yehoshafati akamwambia mfalme wa Israeli, "Tafadhali tafuta mwongozo kutoka
neno la BWANA juu ya kile unachopaswa kufanya kwanza." 6 Ndipo mfalme wa
Israeli akawakusanya manabii pamoja, walikuwa wanaume elfu nne, akawaambia,

“Je, niende Ramothi Gileadi kupigana, au nisiende?” Nao wakamwambia, “Ivamie,
kwa kuwa Bwana ataitoa katika mkono wa mfalme.” 7 Lakini Yehoshafati akasema,
“Je, hapa hayupo nabii mwingine wa BWANA ambaye tunaweza kupata ushauri?”
8 Mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati, “Bado kuna mtu mmoja ambaye
tunaweza kupata ushauri toka kwa BWANA ili kusaidia, Makaya mwana wa Imla,
lakini namchukia kwa sababu huwa hanitabirii mazuri yanayonihusu, ila hunitabiria
matatizo tu.” Lakini Yehoshafat akasema, “mfalme na asiseme hivyo,” 9 Kisha mfalme
wa Israeli akmwita akida na akamwamuru, “Kamlete Makaya mwana wa Imla, sasa
hivi.” 10 Wakati huo Ahabu mfalme wa Israeli na Yehoshafati mfalme wa Yuda
walikuwa wameketi kila mmoja kwenye kiti cha enzi, wamevaa mavazi yao, katika
eneo la wazi kwenye lango la kuingilia Samaria, na manabii walikuwa wakiwatabiria.
11 Sedekia mwana wa Kenaana akajitengenezea pembe za chuma akasema, “BWANA
asema hivi: 'Kwa hili utawasukuma Washami mpaka watakapoisha.'” 12 Na manabii
wengine wote wakasema hivyo, wakisema, “Ishambulie Ramothi Gileadi na ushinde,
kwa kuwa BWANA ameiweka kwenye mkono wa mfalme.” 13 Yule mjumbe aliyeenda
kumwita Makaya akamwambia, akisema, “Tazama sasa, maneno ya manabii kwa
kinywa kimoja wanatabiri mambo mema kwa mfalme. Tafadhali maneno yako
yawe kama yao ukaseme mambo mazuri.” 14 Makaya akajibu, “Kama BWANA
aishivyo, kile BWANA atakachosema kwangu ndicho nitakachosema.'” 15 Naye
alipokuja kwa mfalme, mfalme akamwambia, “Makaya, je twende Ramothi Gileadi
kupigana, au tusiende?” Makaya akamjibu, “Ivamie na ushinde. BWANA ataitoa
kwenye mkono wa mfalme.” 16 Kisha mfalme akamwambia. “Je, nikutake mara
ngapi ili kuniapia ukweli kwa jna la BWANA?” 17 Makaya akasema, “Ninaiona
Israeli yote imesambaa kwenye milima, kama kondoo wasiokuwa na mchungaji,
na BWANA amesema, 'Hawa hawana mchungaji. Kila mtu na arudi nyumbani
kwake kwa amani.'” 18 Kwa hiyo mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati, “Je
sikukwambia kuwa huwa hanitabirii mambo mema yanayonihusu, ila majanga tu?”
19 Kisha Makaya akasema, “Kwa hiyo sikiliza neno la BWANA: Nimemwona BWANA
akiwa ameketi kwenye kiti chake cha enzi, na majeshi yote ya mbinguni yalikuwa
yamesimama karibu yake upande wake wa kulia na upande wake wa kushoto.
20 BWANA akasema, 'Ni nani atakayemdanganya Ahabu, ili kwamba apande akafie
Ramothi Gileadi? Na mtu mmoja akajibu kwa njia hii, na mwingine akajbu kwa
njia ile. 21 Ndipo pepo moja akajitokeza, akasimama mbele ya BWANA, akasema,
'Mimi nitamdanganya.' BWANA akmwuliza, 'Kwa jinsi gani?' 22 Yule pepo akamjibu,
'Nitakwenda na kuwa roho idanganyayo katika vinywa vya manabii wake,' BWANA
akamjibu, 'utaweza kumdanganya, na utafanikiwa. Nenda sasa ukafanye hivyo.'
23 Tazama sasa, BWANA ameweka roho idangayo kwenye vinywa vya hawa manabii
wako, na BWANA ametangaza janga kwako.” 24 Kisha Sedekia mwana wa Kenaana,
akaja, akamzabua Makaya shavuni, akasema, “Je, yule roho wa Bwana alitokaje
kwangu ili asema na wewe?” 25 Makaya akasema, “Tazama, “utatambua hilo
katika siku hiyo, utakapokimbilia katika chumba cha ndani kujificha.” 26 Mfalme
wa Israeli akamwambia mtumishi wake, “Mkamate Makaya umpeleke kwa Amoni,
liwali wa mji, na kwa mwanangu, Yoashi. 27 Mwambie, 'mfalme anasema mweke
huyo gerezani na awe anampa mkate kidogo na maji kidogo, mpaka nitakaporudi
salama.'” 28 Naye Makaya akasema, “Kama utarudi salama basi BWANA hajasema
kupitia kinywa changu.” Na akaongeza, “Sikilizeni hili, ninyi watu.” 29 Ahabu,
mfalme wa Israeli, na Yehoshafati mfalme wa Yuda, wamepanda Ramothi Gileadi.
30 Mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati, “Nitajibadilisha mwenyewe niende
vitani, lakini wewe uvae vazi lako la kifalme.” Kwa hiyo mfalme wa Israeli
akajibadilisha na akaenda vitani. 31 Naye mfalme wa Shamu alikuwa amewaamuru

majemedari thelathini na mbili wa magari yake, akisema, “Msimwamgamize askari
wa muhimu au ambaye si wa muhimu, badala yake mshambulieni mfalme wa Israeli
tu.” 32 Ikawa wakati majemedari wa magari walipomwona Yehoshafati wakasema,
“Hakika huyu ndiye mfalme wa Israeli.” Wakageuka ili kumshambulia, kwahiyo
Yehoshafati akapiga kelele. 33 Ikawa majemedari wa magari walipoona kuwa yeye
hakuwa mfalme wa Israeli, wakamwacha. 34 Lakini mtu mmoja akavuta upinde
wake kwa kubahatisha na akampiga mfalme wa Israeli katikati ya mwunganiko
wa mavazi yake ya chuma. Ahabu akamawambia dereva wa gari lake, “geuza
unirudishe kutoka vitani, kwa kuwa nimeumizwa sana.” 35 Vita ikawa mbaya
sana siku hiyo na mfalme akalazwazwa garini mwake akiwakabili Washami. Akafa
jioni hiyo. Damu ilimwagika kutoka kwenye jeraha lake ndani ya gari. 36 Ikawa
wakati wa kuzama jua, kilio kikatawala kwa jeshi lote, wakisema, “Kila mtu arudi
kwenye mji wake; na kila mtu arudi kwenye mkoa wake!” 37 Kwa hiyo mfalme
Ahabu akafa na akaletwa Samaria, wakamzika huko Samaria. 38 Wakaliosha lile
gari kwenye birika la Samaria, na mbwa wakaramba damu yake (hapa ni mahali
ambapo makahaba waliogea), kama vile neno la BWANA lilivyokuwa limesema.
39 Kwa mambo mengine yanayohusisana na Ahabu, yote ambayo alifanya, ile nyumba
ya pembe aliyojenga, na miji yote aliyojenga, je, hayakuandikwa kwenye kitabu cha
matukio cha wafalme wa Israeli? 40 Kwa hiyo Ahabu akalala pamoja na mababu zake,
na Ahaziya mwanae akawa mfalme mahali pake. 41 Kisha Yehoshafati mwana wa Asa
alianza kutawala juu ya Yuda katika mwaka wa nne wa Ahabu mfalme wa Israeli.
42 Yehoshafati alikuwa na umri wa miaka thelathini na tano alipoanza kutawala, na
akatawala Yerusalemu kwa miaka ishirini na mitano. Mama yake alikuwa Azuba,
binti wa Shilhi. 43 Akatembea katika njia za Asa, baba yake, hakuziacha; akafanya
yaliyokuwa mema mbele ya macho ya BWANA. Lakini bado mahali pa juu palikuwa
hapajabomolewa. Watu walikuwa bado wanaendelea kutoa dhabihu na kufukiza
uvumba mahali pa juu. 44 Yehoshafati akafanya amani na mfalme wa Israeli. 45 Kwa
mambo mengine kuhusiana na Yehoshafati, na nguvu zake alizoonyesha, na jinsi
alivyopigana vita, je, hayajaandikwa katika kitabu cha matukio cha wafalme wa
Israeli? 46 Aliwaondoa kutoka katka nchi wale makahaba wa kipagani waliokuwa
wamebaki katika siku za baba yake Asa. 47 Hapakuwepo mfalme katika Edomu
isipokuwa kaimu mtawala. 48 Yehoshafati alijenga merikebu: ziende Tarshishi
na Ofri kuleta dhahabu, lakini hazikusafiri kwa sababu zile merikebu zilivunjika
kule Esioni Geberi. Kisha 49 Ahazia mwana wa Ahabu akamwambia Yehoshafati,
“Naomba watumishi wangu waende pamoja na watumishi wako merikebuni. “Lakini
Yehoshafati hakuruhusu hilo. 50 Yehoshafati akalala na mababu zake na akazikwa
pamoja nao katika mji wa Daudi, babu yake; Yoramu mwanawe akawa mfalme
mahali pake. 51 Ahazia mwana Ahabu alianza kutawala juu ya Israeli ya Samaria
katika mwaka wa kumi na saba wa mfalme Yehoshafati mfalme wa Yuda, na
akatawala kwa mika miwili juu ya Israeli. 52 Naye akafanya yaliyo maovu mbele ya
macho ya BWANA akatembea katika njia za baba yake, katika njia za mama yake na
katika njia za Yeroboamu mwana wa Nebati, ambazo kwazo aliifanya Israeli kufanya
dhambi. 53 Alimtumikia Baali na kumwabudu na kwa hiyo akamghadhabisha
BWANA, Mungu wa Israeli, katika hasira, kama vile baba yake alivyofanya.

# 2 Wafalme

1 Moabu aliasi dhidi ya Israeli baada ya kifo cha Ahabu. 2 Baada hapo Ahazi
akaanguka chini ya dirisha lenye waya zinazikinzana kwenye chumba chake juu
katika Samaria, na alikuwa amejeruhiwa. Kwa hiyo alituma wajumbe na kuwaambia,
“Nendeni, muulizeni Baal Zebubu, mungu wa Ekroni, kama nitapona hili jeraha.”
3 Lakini malaika wa Yahwe wakamwambia Eliya Mtishbi, “ Inuka, nenda ukaonane
na wajumbe wa mfalme wa Samaria, na uwaulize, 'Je ni kwasababu hakuna
Mungu katika israeli ambaye mnayekwenda kuuliza pamoja na Zebebu, mungu wa
Ekroni? 4 Kwa hiyo Yahwe anasema, “Hutaweza kushuka chini kutoka kwenye
kitanda ambacho ulichokipanda; badala yake, utakufa hakika."”” Baada ya hapo
Eliya akaondoka. 5 wakati wale wajumbe waliporudi kwa Ahazia, akawaambia,
“Kwa nini mmerudi?” 6 Wakamwambia, “mtu amekuja kuonana na sisi ambaye
ametuambia, 'Turudi kwa mfalme ambaye aliyewatuma, na mkamwambie, Yahwe
amesema hivi: 'Je ni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli mpaka mmewatuma
watu kwenda kumuuliza kwa Baal Zabubu, mungu wa Ekron? Kwa hiyo hutashuka
kutoka kitanda ulichokipanda; badala yake, utakufa hakika."”” 7 Ahazi akawaambia
wajumbe wake, “'Alikuwa mtu wa aina gani, yule ambaye alikuja kuonana na ninyi
na akasema haya maneno kwenu?” 8 Wakamjibu, “Alikuwa amevaa kanzu yenye
manyaya na alikuwa na mkanda wa ngozi kiunanoni kwake.'” Hivyo mfalme akajibu,
'“Yule alikuwa Eliya Mtishbi.” 9 Ndipo mfalme akatuma nahodha wa askari hamsini
kwa Elya. Nahodha akaenda mpaka kwa Eliya ambapo alipokuwa amekaa juu ya
mlima. Nahodha akamwambia Eliya, “ Wewe, mtu wa Mungu, mfalme amesema,
'shuka chini.'” 10 Eliya akajibu na kusema kwa nahodha, “Kama mimi ni mtu wa
Mungu, moto na ushuke chini kutoka mbinguni na kukula wewe na watu wako
hamsini.” Kisha moto ukashuka chini kutoka mbinguni na kumla yeye na watu wake
hamsini. 11 Tena Mfalme Ahazi akamtuma nahodha mwingine pamoja na maaskari
wengine hamsini. Huyu nahodha pia akasema kwa Eliya, “Wewe, mtu wa Mungu,
mfalme anasema, teremka chini haraka.”' 12 Eliya akajibu na kuwaambia, “Kama
mimi ni mtu wa Mungu, ngoja moto ushuke kutoka mbinguni na ukule wewe na
watu wako hamsini.” Moto wa Mungu ukashuka chini tena kutoka mbinguni na
kumla yeye na watu wake hamsini. 13 Bado tena mfalme alituma kundi la tatu
la wapiganaji hamsini. Huyu nahodha akaenda, akaanguka mbele ya miguu ya
Eliya, na kumsihi na kumwambia, “Wewe, mtu wa Mungu, Nakuomba, acha uzima
wangu na uzima wa hawa watumishi wako hamsini uwe na thamani machoni kwako.
14 Ndipo, moto ukashuka chini kutoka mbinguni na kuwala wale manahodha wawili
wa kwanza pamoja na watu wao, bali sasa acha uzima wangu uwe na thamani
machoni kwako.” 15 Malaika wa Yahwe akamwambia Eliya, “'Nenda chini pamoja
naye. Usimwogope.”' Hivyo Eliya akainuka na kwenda chini pamoja naye kwenda
kwa mfalme. 16 Baadye Eliya akamwambia Ahazia, '“Hivi ndivyo Yahwe asemavyo,
Umewatuma wajumbe kuzungumza pamoja na Baal-Zebubu, mungu wa Ekron. Je
ni kwa sababu hakuna Mungu katika Israeli ambaye unayeweza kumuuliza habari?
Kwa hiyo sasa, hutaweza kushuka chini kutoka kwenye kitanda ulichokipanda;
utakufa hakika.'” 17 Hivyo Mfalme Ahazia alikufa kulingana na neno la Yahwe ambalo
Eliya alilisema. Yoramu alianza kutawala katika eneo lake, katika mwaka wa pili
Yoramu mwana wa Yohoshafati mfalme wa Yuda, kwa sababu Ahazia hakuwa na
mtoto. 18 Kama mambo mengine yanayomuhusu Ahazia, je hayakuandikwa katika
kitabu cha matukio ya wafalme wa Israeli?

# 2

1 Hivyo ilipokuja kuhusu, wakati Yahwe alipokuwa akienda kumchukua Eliya
kwenda mbinguni kwa uvumi, ambapo Eliya aliondoka pamoja na Elisha kutoka
Gigali. 2 Eliya akamwambia Elisha, '"kaa hapa, tafadhali, kwa sababu Yahwe
alinituma kwa Betheli.'" Elisha akajibu, "Kama Yahwe aishivyo, na kama uishivyo,
sintokuacha.'" Hivyo wakashuka chini kulekea Betheli. 3 Wana wa manabii ambao
walikuwa Betheli walikuja kwa Elisha na kumwambia, je unajua kwamba Yahwe
atamwondoa bwana wako kuanzia leo?"' Elisha akajibu, "Ndiyo, nalijua hilo, ila
msizungumze kuhusu hilo."' 4 Eliya akamwambia, "Elisha, subiri hapa, tafadhali,
kwa kuwa Yahwe amenituma niende Yeriko." Kisha Elisha akajibu, '"Kama Yahwe
aishivyo, na kama uishivyo, sintokuacha." Hivyo wakaenda Yeriko. 5 Kisha wana
wa manabii ambao walikuwa Yeriko wakaja kwa Elisha na kumwambia, "'Je unajua
kwamba Yahwe atamwondoa bwana wako kutoka kwako leo?" Elisha akajibu,
"Ndiyo, nalijua hilo, lakini msilizungumzie hilo." 6 Kisha Eliya akamwambia, '"kaa
hapa, tafadhali, kwa kuwa Yahwe amenituma kwenda Yeriko." Elisha akajibu, "Kama
Yahwe ishivyo, na kama uishivyo, sintokuacha." Hivyo wawili wakaenda mbele.
7 Baadaye watu hamsini wa watoto wa wale manabii wakasimama kuwakabili kwa
mbali kidogo wale wawili wakasimama karibu na Yordani. 8 Eliya akachukua vazi
lake, akaliviringisha, na kuyapiga maji kwa kutumia lile vazi. Ule mto ukagawanyika
katika sehemu mbili hivyo basi wawili hao wakatembea hadi nchi kavu. 9 Ilitokea,
walipokwisha kuvuka, kwamba Eliya akamwambia Elisha, "Niambie unachotaka
nifanye kwako kabla sijaondolewa kutoka kwako." Elisha akajibu, "Naomba sehemu
kubwa ya roho yako ije kwangu. 10 Eliya akajibu, "Umeomba jambo gumu. Hata
hivyo, kama ukiniona wakati nitakapoondolewa kutoka kwako, hii itatokea kwako,
lakini kama sivyo, haitatokea." 11 Ikawa walipokuwa bado wakienda mbele na
kuzungumza, gari la kukokotwa na farasi lenye moto na farasi wa moto ikatokea,
ambapo iliwatenga wale watu wawili kutoka kila mmoja, na Eliya akaenda juu
kwa uvumi wa upepo kwenda mbinguni. 12 Elisha akaiona akalia kwa sauti,
"Baba yangu, baba yangu, gari la kukokotwa na farasi la Israeli na waendesha
farasi!'" Hakumwona Eliya tena, na akashikilia nguo zake mwenyewe na kugawanya
kwenye vipande viwili. 13 Akachukua vazi la Eliya lililokuwa limemwangukia, na
kurudi kusimama kwenye ukingo wa Yordani. 14 Akayapiga maji pamoja na lile
vazi la Eliya alilokuwa ameliangusha na kusema, "Yahwe yuko wapi, Mungu wa
Eliya?'" Wakati alipoyapiga yale maji, yaligawanyika katika pande mbili na Elisha
akavuka. 15 Wakati hao wana wa manabii ambao walitoka Yeriko walipomuona
akikatiza kwao, wakasema, "roho ya Eliya imepumzika kwa Elisha!" Hivyo wakaja
kuonana naye, na wakasujudu aridhini mbele yake. 16 Wakamwambia, "Ona sasa,
miongoni mwa watumishi wako kuna watu hamsini hodari. Tunakuomba Waache
waende, na kumtafuta bwana wako, endapo huyo Roho wa Yahwe alipomchukua
juu na kumtupa juu ya mlima mmoja au kwenye bonde moja." Elisha akajibu,
"Hapana, msiwatume." 17 Lakini walimsihi Elisha hadi akaona aibu, akasema,
"Watume."Ndipo wakawatuma watu hamsini, na wakatafuta kwa mda wa siku tatu,
lakini hawakumpata. 18 Wakarudi kwa Elisha, wakati alipokuwa bado yuko Yeriko,
na akasema, "Je sikusema, 'msiende'?" 19 Watu wa mjini wakamwambia Elisha,
"Ona, tunakuomba, hali ya mjini hapa ni pazuri, kama bwana wangu awezavyo
kuona, lakini maji ni mabaya na hiyo nchi haiwezi kuzaa matunda." 20 Elisha
akajibu, "Nileteeni bakuli jipya na muweke chumvi ndani ya hilo bakuli," hivyo
wakamletea. 21 Elisha akaenda hadi kwenye chemichemi za maji na kutupia chumvi
ndani; halafu akasema, "Yahwe asema hivi, 'Nimeyaponya haya maji. Kuanzia mda
huu, hakutakuwa na kifo au nchi isiyozaa matunda. 22 "Hivyo hayo maji yakaponya

hata leo, kwa lile neno ambalo Elisha aliongea. 23 Ndipo Elisha akapanda kutoka
pale mpaka Betheli. Naye alipokuwa akienda hadi kwenye barabara, wakatokea
vijana nje ya mji na kumtania, wakamwambia, “Panda juu, wewe mwenye kipara!
Panda juu, wewe mwenye kipara!” 24 Elisha alipotazama nyuma yake na kuwaona;
alimwambia Yahwe awalaani. Ndipo dubu wa kike wawili wakatokea kichakani na
kuwajeruhi vijana arobaini na mbili. 25 Ndipo Elisha alipoondoka pale na kuelekea
Mlima Karmeli, na kutoka huko alirudi samaria.

# 3

1 Basi katika mwaka wa kumi na nane wa Yehoshefati mfalme wa Yuda, Yoramu
mwana wa Ahabu alianza kutawala juu ta Israeli katika Samaria; alitawala miaka
kumi na miwili. 2 Alifanya yaliyo maovo usoni kwa Yahwe, lakini si kama baba yake
na mama yake; kwa kuwa aliiondoa ile nguzo ya mungu wa Baali ambayo baba
yake aliitengeneza. 3 Hata hivyo alishikilia dhambi za Yeroboamu mwana wa Nebati,
ambaye alisababisha Israeli kufanya dhambi; wala hakuziacha mbali nao. 4 Basi
Mesha mfalme wa Moabu alifuga kondoo. Alikuwa akimpatia mfalme wa Israeli
kondoo 100, 000 na manyoya ya kondoo dume 100, 000. 5 Ila baada ya Ahabu kufa,
yule mfalme wa Moabu aliasi dhidi ya mfalme wa Israeli. 6 Hivyo Mfalme Joramu
alikaondoka Samaria katika muda huo kuwahamasisha Waisraeli wote kwa ajili ya
vita. 7 Akatuma mjumbe kwa Yehoshafati mfalme wa Yuda, akisema, “Mfalme wa
Moabu ameasi dhidi yangu. Je mtakwenda pamoja nami kupigana dhidi ya Moabu?”
Yehoshafati akajibu, “Nitaenda. Mimi ni kama wewe, watu wangu ni kama watu
wako, farasi wangu ni kama farasi wako.” 8 Ndipo akasema, “Tutawashambulia
kwa njia gani?” Yehoshafati akajibu, “Kwa njia ya jangwa la Edemu. 9 Hivyo
huyo mfalme wa Israeli, Yuda, na Edomu wakazunguka kwa mda wa siku saba.
Hapakuwa na maji kwa ajili ya jeshi lao, wala kwa farasi au wanyama. 10 Basi mfalme
wa Israeli akasema, “Hii ni nini? Yahwe amewaita wafalme watatu ili kutekwa
mikononi mwa Moabu?” 11 Lakini Yehoshafati akasema, “je hakuna nabii wa Yahwe,
ambaye tunaweza kufanya shauri kuhusu Yahwe kupitia yeye?” Mtumishi mmoja wa
wafalme wa Israeli akajibu na kusema, “Elisha mwana wa Shafati yuko hapa, ambaye
alikuwa akimimina maji kwenye mikono ya Eliya.” 12 Yehoshafati akasema, “Neno
la Yahwe liko pamoja nami.” Hivyo mfalme wa Israeli, Yehoshaphati, na mfalme
wa Edomu wakashuka chini kwenda kwake. 13 Elisha akamwambia mfalme wa
Israeli, “Nifanye nini kwa ajili yako? Nenda kwa manabii wa baba na mama yako.”
Ndipo mfalme wa Israeli akamwambia, “Hapana, kwa sababu Yahwe amewaita
hawa wafalme watatu pamoja ili kuruhusu jeshi la Moabu liwateke.” 14 Elisha
akajibu, “Kama Yawhe wa majeshi aishivo, ambaye nimesimama mbele zake, hakika
kama nisingemheshimu uwepo wa Yehoshafati mfalme wa Yeda, Nisingevuta usikivu
kwako, au hata kukutazama. 15 Lakini sasa niletee mwanamuziki.” Ndipo alipokuja
mpiga muziki alipocheza, mkono wa Yahwe ukaja juu ya Elisha. 16 Akasema, “'Yahwe
asema hivi, 'Fanya hili bonde la mto mkavu lijae mahandaki.' 17 Kwa kuwa Yahwe
asema hivi, 'Hutaona upepo, wala hamtaona mvua, bali hili bonde la mto litajaa maji,
na mtakunywa, ninyi na mifugo yenu na wanyama wenu wote.' 18 Hiki ni kitu rahisi
usoni mwa Yahwe. Pia atawapa ushindi juu ya hao Wamoabu. 19 Mtaiteka kila ngome
ya mji na kila mji mzuri, kukata kila mti mzuri, kusimamisha chemichemi zote za
maji, na kuharibu kila sehemu nzuri ya nchi na miamba.” 20 Hivyo asubuhi karibia
na mda wa kutoa sadaka ya kuteketeza, yakaja maji kutoka uelekeo wa Edomu;
nchi ikajaa maji. 21 Ndipo wakati Wamoabu wote waliposikia kwamba wafalme
wamekuja kupigana dhidi yao, walikusanyika pamoja, wote waliotakiwa kubeba
silaha, na wakasimama mpakani. 22 Walitembea asubuhi na mapema na jua likang'aa

kwenye maji. Wakati Wamoabu walipoyaona yale maji yaliyowaelekea, yanaonekana
mekundu kama damu. 23 Wakatamka kwa hasira, “Hii ni damu! Yamkini hao
wafalme wameharibiwa, na wameuna wao kwa wao! Sasa basi, Moabu, ngoja
tuende tukawateke nyara!” 24 Wakati walipokuja kwenye kambi ya Israeli, Waisraeli
wakawashtukiza na kuwashambulia Wamoabi, ambao walikimbia mbele yao. Hilo
jeshi la Israeli waliwakimbiza hao Wamoabu hadi kwao wakiwaua. 25 Waliiharibu
miji, na kila aina ya amani ya nchi kila mtu alirusha jiwe mpaka ulipojaa. Walizuia
kila chemichemi ya maji na kukata chini miti mizuri yote. Kir-haresethi tu ndiyo
ilichwa na mawe yake. Lakini hao maaskari wakawashambulia na makombeo
wakiwazunguka na kuishambulia. 26 Ndipo Mfalme Mesha wa Moabu alipoona
kwamba ameshindwa, alichukua watu hodari wa upanga mia saba pamoja naye
kwenda kwa mfalme wa Edomu, lakini walishindwa. 27 Ndipo akamchukua mtoto
wake wa kwanza, ambaye angetawala baada ya yeye, na akamuudhi kwa kumtoa
kama sadaka ya kuteketezwa juu ya ukuta. Hivyo, kulikuwa na hasira kubwa dhidi
ya Israeli, na hao Waisraeli, na Jeshi la Israeli likamuacha mfalme Mesha na kurudi
kwenye nchi yao.

# 4

1 Ndipo mke wa mmoja wa watoto wa manbii alipokuja kwa Elisha akilia, akisema,
“Mtumishi wako mme wangu amukufa, na unajua kwamba mtumishi wako alikuwa
anamcha Yahwe. Basi aliyemuwia amekuja kuwachukua watoto wangu wawili
kwenda kuwa watumwa.” 2 Hivyo Elisha akamwambia, “Nikusaidie nini? Niambie
una nini kwenye nyumba yako?” Akamwambia “Mtumishi wako hana kitu kwenye
nyumba, isipokuwa chupa ya mafuta.” 3 Kisha Elisha akasema, “Nenda kaazime
vyombo kwa majirani zako, vyombo vitupu. Azima vyombo vingi uwezavyo. 4 Kisha
lazima uende ndani na kujifungia mlango wewe na watoto wako, na kumiminia
mafuta vyombo vyote; vile vilivyojaa ukavitenge.” 5 Basi akamuacha Elisha na
kujifungia mlango yeye na watoto wake. Wakavileta vile vyombo kwake, na akivijaza
kwa mafuta. 6 Ikawa vyombo vilipojaa, akamwambia mtoto wake, “Niletee chombo
kingine.” Ila akamwambia, “Hakuna vyombo vingine.” Kisha mafuta yakakoma
kutoka. 7 Ndipo akaja na kumwambia mtu wa Mungu. Akasema, “Nenda kauze
mafuta; lipa deni lako, na yatakayobaki waachie watoto wako.” 8 Siku moja
Elisha alitembea Shunemu ambapo mwanamke muhimu aliishi; alimsihi ale chakula
pamoja naye. Ikawa alipopita mara nyingi, angeweza kusimama pale na kula. 9 Huyo
mwanamke akamwambia mme wake, “Ona, sasa nadhani kwamba huyu ni mtu
mtakatifu wa Mungu ambaye hupita siku zote. 10 Ngoja tutengeneze chumba kidogo
kwenye paa kwa ajili ya Elisha, na tuweke kitanda juu ya hicho chumba, meza, na taa.
Kisha atakapokuwa anakuja kwetu, atakuwa anakaa hapo.” 11 Ikawa siku moja akaja
tena kwamba Elisha akasimama pale, akakaa kwenye hicho chumba na kupumzika
hapo. 12 Elisha akamwambia Gehazi mtumishi wake, “Mwite huyu Mshunami.”
Wakati alipomuita, alisimama mbele yake. 13 Elisha akamwambia, “Mwambie,
'Umetusumbukia kwa kutujali. Nini kifanyike kwa ajili yako? Tunaweza kukuombea
kwa mfalme au amri jeshi?”” Akajibu, “Ninaishi miongoni mwa watu wangu.”
14 Kisha Elisha akajibu, “Tumfanyie nini kwa ajili yake, sasa?” Gehazi akajibu, “Kweli
hana mtoto, na mume wake ni 15 mzee.” Hivyo Elisha akajibu, “Mwite.” Wakati
alipomuita, akasimama kwenye mlango. 16 Elisha akasema, “Katika kipindi kama
hiki mwakani, katika kipindi cha mwaka mmoja, utakuwa ukimkumbatia mtoto.”
Akasema “Hapana, bwana wangu na mtu wa Mungu, usidanganye kwa mtumishi
wako.” 17 Lakini yule mwanamke akabeba mimba na kujifungua mtoto wakume
kipindi hicho hicho katika mwaka uliofuata, kama Elisha alivyokuwa amemwambia.

[18] Wakati mtoto alipokuwa mkubwa, akaenda kwa baba yake siku moja, ambaye
alikuwa na watu wanaovuna. [19] Akamwambia baba yake, "Kichwa changu, kichwa
changu." Baba yake akamwambia mtumishi wake, "Mbebe mpeleke kwa mama
yake." [20] Wakati mtumishi alipombeba kumrudisha kwa mama yake, yule mtoto
alikaa kwenye magoti yake hadi mchana na baada ya hapo mtoto alikufa. [21] Hivyo
yule mwanamke akambeba na kumlaza kwenye kile kitanda cha mtu wa Mungu,
akafunga mlango, na kutoka nje. [22] Akamwita mume wake, na kusema, "Tafadhali
nitumie mmoja wa watumishi wako na moja ya punda wako ili niweze kuwahi kwa
mtu wa Mungu ili niweze kurudi." [23] Mume wake akasema, "Kwa nini unataka
kwenda kwake leo? Sio mwezi mpya wala Sabato." alijibu, "Itakuwa sawa." [24] Ndipo
akatandika kwenye punda na kumwambia mtumishi wake, "Mwendeshe haraka;
usinipunguzie mwendo hadi nitakapokwambia ufanye hivyo." [25] Hivyo aliendа
na kuja na mtu wa Mungu katika mlima Karmeli. Basi wakati mtu wa Mungu
alipomuona kwa mbali, akamwambia Gehazi mtumishi wake, "Tazama, mwanamke
Mshunami anakuja. [26] Tafadhali mkimbilie na umwambie, 'Hamjambo kwako pamoja
na mume wako na mtoto wako?" Akajibu, "Hawajambo." [27] Baada ya kufika kwa
huyo mtu wa Mungu katika mlima, alimkumbatia miguu yake. Gehazi akaja karibu
ili kumuondoa lakini mtu wa Mungu akasema, "Muache, kwa kuwa amefadhaika
sana. na Yahwe amenificha tatizo kwangu, na hajanambia kitu." [28] Ndipo aksema,
"Nilikuuliza mtoto wako, bwana wangu? Sikusema, 'Usinifiche'? [29] Ndipo Elisha
akamwambia Geahazi, "Vaa kwa ajili ya safari na uchukue fimbo yangu mkononi
mwako. Nenda kwake. Kama ukimkuta mtu yeyote, usimsalimie, na kama mtu
yeyote akikusalimia, usimjibu. Laza fimbo yangu kwenye uso wa mtoto. [30] Lakini
mama yake na huyo mtoto akasema, "Kama Yahwe aishivyo, na kama uishivyo,
sintokuacha." Hivyo Elisha akainuka na kumfuata. [31] Gehazi akawatangulia na
kulaza ile fimbo kwneye uso wa yule mtoto, lakini yule mtoto hakuongea wala
kusikia. Hivyo baada ya hapo Gehazi akarudi kuonana na Elisha na kumwambia
akisema, "Mtoto hakuamka." [32] Ndipo Elisha alipofika kwenye ile nyumba, yule
mtoto alikuwa amekufa na alikuwa bado yupo kwenye kitanda. [33] Hivyo Elisha
aliingia ndani na kufunga malango yeye mwenyewe na yule mtoto na kuomba kwa
Yahwe. [34] Alipanda juu na kulala juu ya yule mtoto; aliweka mdomo wake kwenye
mdomo wake, macho yake kweneye macho yake, na mikono yake kwenye mikono
yake. Akajinyoosha yeye mwenyewe kwa yule kijna, na mwili wa yule mtoto ukaanza
kupata joto. [35] Baada ya hapo Elisha aliinuka na kuanza kutembea kuzunguka kile
chumba na kurudi tena juu na kujinyoosha mwenyewe kwa yule kijana. Yule kijana
alipiga chafya mara saba na kisha akafungua macho yake! [36] Hivyo Elisha akamwita
Gehazi na kumwambia, "Mwite yule Mshunami!" Hivyo akamwita, na wakati
alipofika kwenye kile chumba, Elisha akasema, "Mchukue mtoto wako." [37] Kisha
akainamisha uso wake chini kwenye miguu yake na kusujudu, na kisha kumchukua
mtoto wake na kuondoka. [38] Kisha Elisha akarudi tena Gilgali. Kulikuwa na njaa
katika nchi, na wana wa manabii walikuwa wamekaa mbele yake. Akamwambia
mtumishi wake, "Weka sufuria kubwa kwenye moto na pika kwa ajili ya watoto
wa manabii." [39] Mmoja wao akaenda kwenye shamba kukusanya mboga mboga.
Alikuta matango ya porini na kukusanya ya kutosha hadi alipojaza kwenye nguo
yake. Walizikata na kuziweka kwenye sufuria, lakini hakujua zilikuwa za aina gani.
[40] Basi, wakawapakulia na kusambaziwa kwa watu kwa ajili ya kula. Baadae, kadiri
walivyokuwa wakiendelea kula, walipiga kelele na kusema, "Mtu wa Mungu, kuna
kifo kwenye sufuria!" Hivyo wasingeweza kula tena. [41] Lakini Elisha akasema, "Late
unga." Alitupia kwenye sufuria na kusema, "Pakua kwa watu kwa ajili ya kula, kwa
hiyo wanaweza kula." Kisha hapakuwa kitu chochote kibaya kwenye ile sufuria.

42 Akaja mtu kutoka Baal Shalisha kwa mtu wa Mungu na kumletea chakula cha
kwanza cha mavuno yake mikate shirirni ya shayiri, na masuke mabichi kwenye
gunia. Akasema, “Wape haya watu ili waweze kula.” 43 Mtumishi wake akasema, “Je,
niandae hii mbele ya watu mia moja?” Lakini Elisha akasema, “Wapeni hawa watu,
ili waweze kula, kwa sabau Yahwe anasema, 'Watakula na kingine kitabaki.”' 44 Basi
mtumishi wake akawaandalia mbele yao; wakala, na kuacha kingine kimebaki, kama
neno la Yahwe lilivyokuwa limesema.

# 5

1 Basi Naamani, amri jeshi wa mfalme wa Shamu, alikuwa mtu mkubwa na
mtu mwenye kuheshimiwa mbele ya bwana wake, kwa sababu kwa ajili yake
Yahwe aliwapa ushindi Washami. Pia alikuwa hodari, mtu shujaa, lakini alikuwa
anaukoma. 2 Washami walikuwa wametoka kuongoza kikosi na kumchukua kijana
mdogo wa kike kutoka nchi ya Israeli. Akamuhudumia mke wa Naamani. 3 Yule
binti akamwambia bibi yake, “Natamani kwamba bwana wangu angelikuwa na
nabii ambaye yupo Samaria! Halafu angelimponya bwana wangu ukoma wake.
4 Hivyo Naamani akaingia na kumwambia mfalme kile ambacho yule binti kutoka
nchi ya Israeli alichokuwa amekisechosema. 5 Kisha mfalme wa Shamu akase,
“Nenda sasa, na nitatuma barua kwa mfalme wa Israeli.” Naamani akaondoka na
kuchukua talanta zake kumi za fedha, vipande elfu sita vya dhahabu, na nguo kumi
za kubadilisha. 6 Pia alichukua barua ya kumpelekea mfalme wa Israeli inayosema,
“Sasa wakati hii barua itakapoletwa kwako, utaona kwamba nimemtuma mtumishi
wangu Naamani kwako, hivyo basi utamponya ukoma wake.” 7 Wakati mfalme
wa Israeli alipoisoma ile barua, alichana mavazi yake na kusema, “Je mimi ni
Mungu, niue na nirudishe uhai, kwamba huyu mtu anataka nimponye mtu ukoma
wake? Inaonekana anatafuta mashindano na mimi.” 8 Ikawa wakati Elisha mtu
wa Mungu aliposikia kwamba mfalme wa Israeli alichana nguo zake, akatuma neno
kwa mfalme akisema, “Kwa nini umechana nguo zako? Muache aje kwangu sasa,
na atajua kwamba kuna nabii katika Israeli.” 9 Basi Naamani akaja na farasi
wake na mikokoteni yake ya kukokotwa na farasi na kusimama kwenye mlango
wa nyumba ya Elisha. 10 Elisha akamtumia mjumbe, akisema, “Nenda na ukazame
mwenyewe katika Yordani mara saba, na ngozi ya mwili wako itajirudi; utakuwa
msafi.” 11 Lakini Naamani alikasirika na kuondoka na kusema, “Tazama, Nilidhani
bila shaka angekuja kwangu na kusimama na kuliita jina la Yahwe Mungu wake,
na kupitisha mkono wake kwenye sehemu ya ugonjwa na kuponya ukoma wangu.
12 Je sio Abana na Faepari, mito ya Damaskasi, bora kuliko maji yote ya Israeli?” Je
siwezi kuoga ndani yao na kuwa safi?” Hivyo akageuka na kwenda kwa hasira.
13 Ndipo watumishi wa Naamani wakaja karibbu na kumwambia, “Baba yangu,
kama yule nabii alikuamuru kufanya kitu kigumu, singelifanya? Je si zaidi basi,
atakapokwambia rahisi, 'Zama mwenyewe na uwe safi?” 14 Ndipo akashuka chini na
kuzama mwenyewe mara saba kwenye Yordani, akitii maelekezo ya mtu wa Mungu.
Nyama ya mwili wake ikarudi tena kama nyama ya mwili ya mtoto mdogo, na
alikuwa amepona. 15 Naamani akarudi kwa yule mtu wa Mungu, yeye na watu wake
wengine, na kuja na kusimama mbele yake. Akasema, “Tazama, sasa najua kwamba
hakuna Mungu katika Dunia nzima isipokuwa katika Israeli. Kwa hiyo basi, chukua
zawadi kutoka kwa mtumishi wako tafadhali.” 16 Lakini Elisha akajibu, “Kama
Yahwe aishivyo, ambaye nimesimama mbele yake, sintopokea chochote.”Naamani
akamsihi Elisha apokee zawadi, lakini alikataa. 17 Hivyo Naamani akasema, “Kama
sivyo, nakuomba ache apewe mtumishi wako pale mzigo wa baghala mbili za aridhi,
kwa kuwa kuanzia sasa, mtumishi wako hatotoa tena sadaka ya kuteketezwa wala

dhabihu kwa mungu yeyote isipokuwa Yahwe. 18 Katika jambo hili moja Yahwe
anaweza kumsamehe mtumishi wako, hii ni, wakati mfalme wangu atakapoenda
kwenye nyumba ya Rimoni kuabudu pale, na kujifunza kwenye mikono yangu na
kumuinamia mwenyewe kwenye nyumba ya Rimoni, Yahwe aweze kumsamehe
mtumishi wako katika hili jambo." 19 Elisha akamwambia, "Nenda kwa amani."
Hivyo Naamani akaondoka. 20 Alikuwa amesafiri lakini umbali mfupi, wakati Gehazi
mtumishi wa Elisha mtumishi wa Mungu alisema mwenyewe, "Tazama, bwana
wangu amemuandaa huyu Naamani Mshami kwa kuacha kupokea zawadi kutoka
kwenye mikono yake ambazo alizileta. Kama Yahwe aishivyo, Nitakimbia nikimfuata
na kupokea kitu kutoka kwake. 21 Hivyo Gehazi akamfuata Naamani. Wakati
Naamani alipomuona mtu mmoja anakimbia akimfuata, aliruka chini kutoka kwenye
gari yake kuonana naye na kusema, "Je kila kitu kiko sawa?" 22 Gehazi akasema,
"kila kitu kiko sawa. Bwana wangu amenituma, akisema, 'Tazama, sasa wamekuja
kwangu kutoka nchi ya mlima ya Efraimu vijana wawili wa watoto wa manabii.
Tafadhali, wapatie talanta ya fedha na nguo mbili za kubadilisha." 23 Naamani
akajibu, "Ninafuraha kubwa kukupatia talanta mbili." Naamani akamsihi Gehazi na
kujaribu talanta mbili za fedha kwenye mifuko miwili ya kubebea, pamoja na nguo
mbili za kubadilisha, na kutandaza kwa wafanyakazi wake wawili, ambao walikuwa
wamebebea ile mifuko miwili ya fedha mbele ya Gehazi. 24 Wakati Gehazi alipokuja
kwenye ule mlima, alichukua ile mifuko ya fedha kutoka kwenye mikono yao na
kuificha kwenye nyumba; akawatuma wale watu, na wakaondoka. 25 Wakati Gehazi
alipoingia na kusimama mbele ya bwana wake, Elisha akamwambia, "Umetokea
wapi, Gehazi?" Akajibu, "Mtumishi wako hakwenda mahali." 26 Elisha akamwambia
Gehazi, "Je roho yangu haikuwa na wewe wakati yule mtu alipoyarudisha magari
yake ya farasi ili kukutana na wewe? Je uu ni mda wa kupokea pesa na nguo,
mashamba ya mzaituni na mizabibu, na kondoo na Ng'ombe, na watumishi wakiume
na watumishi wakike? 27 Basi ukoma wa Naamani utakuwa kwenye uzao wako
daima." Basi Gehazi akatoka kwenye uwepo wake, mwenye ukoma kama theluji.

# 6

1 Wana wa manabii wakamwambia Elisha, "Sehemu ambayo tunayoishi na wewe ni
ndogo sana kwa ajili ya wote. 2 Tafadhali, tuache tuende Yordani, na umwache kila
mtu akate mti hapo ambako tunaweza kuishi." Elisha akajibu, "unaweza kwenda
mbele." 3 Mmoja wao akasema, "Nenda na watumishi wako tafadhali." Elisha
akajibu, "Nitaenda." 4 Kwa hiyo akaenda pamoja nao, na wakati walipokuja Yordani,
wakaanza kukata miti. 5 Lakini mmoja wao alipokuwa akikata, kichwa cha shoka
kikaangukia kwenye maji; akalia kwa sauti na kusema, "la hasha, bwana wangu,
kilikuwa kimeazimwa!" 6 Basi mtu wa Mungu akasema, "kiliangukia wapi?" Yule
mtu akamwonyesha Elisha ile sehemu. akakata fimbo, akarusha kwenye maji, na
kufanya chuma kuelea. 7 Elisha akasema, "Kichukue." Basi yule mtu akafikisha
mkono wake na kukinyakua. 8 Basi mfalme wa Shamu alikuwa akipigana vita dhidi
ya Israel. Akafanya shauri na watumishi wake, akisema, "kambi yangu itakuwa
sehemu flani na flani." 9 Basi huyo mtu wa Mungu akamtuma kwa mfalme wa Israeli,
akisema, "Kuwa makini usipite ile sehemu, kwa kuwa ndipo Washamu wanakoshukia
hapo." 10 Mfalme wa Israeli akatuma mjumbe kwenda pale sehemu ambayo mtu
wa Mungu alipaongelea na kumtahadharisha. Zaidi ya mara moja au mbili, wakati
mfalme alipoenda pale, alikuwa kwenye ulinzi wake. 11 Huyo mfalme wa Shamu
alikasirishwa kuhusu haya maonyo, na akawaita watumishi wake na kuwaambia,
"Je hamtaniambia ni nani miongoni mwetu aliye upande wa Israeli?" 12 Hivyo
mmoja wa watumishi wake akasema, "Hapana, bwana wangu, mfalme, kwa ajili ya

Elisha yule nabii katika Israeli humwambia yule mfalme wa Israeli maneno ambayo
uyaongeayo kwenye kitanda chako cha kulala.!" 13 Yule mfalme akajibu, "Nenda
na uone Elisha alipo hivyo naweza kutuma watu na kumkamata." Akaambiwa,
"Tazama yuko Dothani." 14 Kwa hiyo yule mfalme akatuma farasi kwenda Donathi,
magari ya farasi, na jeshi kubwa. Wakaja usiku na kuzunguka ule mji. 15 Wakati
yule mtumishi wa mtu wa Mungu alipoamka mapema na kutoka nje, kumbe, jeshi
kubwa pamoja na farasi na magari ya farasi yameuzunguka mji. Mtumishi wake
akamwabia, "Kumbe, bwana wangu! Tutafanya nini?" 16 Elisha akajibu, "usiogope,
wale walio na sisi ni zaidi kuliko wale walio nao." 17 Elisha akajibu na kusema,
"Yahwe, nakuomba kwamba utamfungua macho yake ili kwamba aweze kuona."
Ndipo Yahwe alipofungua macho ya mtumishi, na akaona. Kumbe, ule mlima ulikuwa
umejaa farasi na magari ya farasi ya moto yamemzunguka Elisha! 18 Wakati hao
Washami walipomshukia chini, Elisha aliomba kwa Yahwe na kusema, "Uwapige
hawa watu kwa upofu, nakuomba." Hivyo Yahwe akawafanya vipofu, kama Elisha
alivyoomba. 19 Kisha Elisha akawaambia Washami, "Hii njia sio, pia mji huu
sio. Nifuateni mimi, na nitawaleta kwa yule mtu ambaye mnayemtafuta." Ndipo
akawaongoza kweda Samaria. 20 Hata walipokwisha kufika Samaria, Elisha akasema,
"Yahwe, fungua macho ya hawa watu ili waweze kuona." Yahwe akawafungua
macho yao na wakaona, na kumbe, walikuwa katikati ya mji wa Samaria. 21 Yule
mfalme wa Israeli akamwambia Elisha, wakati alipowaona, "Baba yangu, niwaue?
Niwaue?" 22 Elisha akajibu, "Usiwaue. Ungeweza kuwaua wale ambao uliokuwa
umewachukua mateka kwa upanga na upinde wako? Weka mkate na maji mbele
yao, ili kwamba waweze kula na kunywa, na kwenda kwa bwana wao." 23 Ndipo
mfalme akaandaa chakula kingi kwa ajili yao, na wakati walipokula na kunywa,
akawapeleka mbali, na walirudi kwa bwana wao. Lile kundi la jeshi la Wasahami
halikurudi kwa mda mrefu katika nchi ya Israeli. 24 Baadaye baada ya huyu Ben
Hadadi mfalme wa Shamu kukusanya majeshi yake yote na kuiteka Samaria na
kuizingira. 25 Hivyo kulikuwa na njaa kubwa katika Samaria. Kumbe, wakauzingira
hadi kichwa cha punda kilipouzwa kwa vipande themanini vya fedha, na sehemu
ya nne ya sehemu ya kibaba cha kinyesi cha njiwa kwa vipande vitano vya fedha.
26 Wakati mfalme wa Israeli alipokuwa akipita karibu na ukuta, mwanamke mmoka
akamlilia akisema, "Nisaidie, bwana wangu, mfalme." 27 Akasema, "Kama Yahwe
hawezi kukusaidia, je nitakusaidiaje? je kuna kitu chochote kinakuja kutoka sehemu
ya kupuria nafaka au shinikizoni?" 28 Mfalme akaendelea, "Nini kinakusumbua?"
Akajibu, "Huyu mwanamke ameniambia, 'Mtoe mtoto wako ili tuweze kumla leo,
na tutamla wakwangu kesho." 29 Hivyo tulimchemsha mtoto wangu na kumla,
na siku ya pili yake nikamwambia, "Mtoe mtoto wako ili tuweze kumla, lakini
alikuwa amemficha mtoto wake." 30 Basi mfalme aliposikia yale maneno ya yule
mwanamke, akayachana mavazi yake (sasa alikuwa akitembelea kwenye ukuta),
na watu wakatazama na kuona kwamba alikuwa amevaa nguo ya gunia chini,
dhidi ya ngozi yake. 31 Kisha akasema, "Mungu afanye hivyo kwangu, na zaidi
pia, kama kichwa cha Elisha mwana wa Shafati kitabaki juu yake leo." 32 Basi
Elisha alikuwa ameketi kwenye nyumba yake, na wazee walikuwa wamekaa pamoja
naye. Yule mfalme akamtuma mtu wa mbele yake, lakini wakati mjumbe alipokuja
kwa Elisha, akawaambia wazee, "Ona jinsi huyu mwana wa muuaji alivytumwa
kuchukua kichwa changu? Tazama, wakati yule mjumbe atakapokuja, funga mlango,
na uushikilie huo mlango funga dhidi yake asiingie. Je sio sauti ya bwana wake
nyuma mguuni pake?" 33 Wakati alipokuwa bado akiongea pamoja nao, kumbe, yule
mjumbe alishuka kwake. Mfalme akasema, "Kumbe, masumbuko haya yatoka kwa
Yahwe. Kwa nini nimsubiri Yahwe tena?"

# 7

1 Elisha akasema, “Sikiliza neno la Yahwe. Hivi ndivyo Yahwe asemavyo: “Kesho
mda kama huu kipimo cha unga mzuri kitauzwa kwa shekeli, na vipimo viwili vya
shayiri kwa shekeli, kwenye lango la Samaria."" 2 Basi yule nahodha ambaye alikuwa
akitegemea mkono wake amemjibu mtu wa Mungu, na kusema, “Ona, hata kama
Yahwe ataweka madirisha mbinguni, je jambo hili linawezekana?” Elisha akajibu,
“Ona, utaona ikitokea kwa macho yako mwenyewe, lakini hutakula chochote katika
hilo.” 3 Basi, kulikuwa na watu wanne wenye ukoma upande wa nje wa lango la mji.
Wakaambizana kila mmoja, “Kwa nini tukae hapa hadi hapo tutakapokufa? 4 Kama
tukisema kwamba tutaenda kwenye ule mji, maana mjini kuna njaa, na tutakufa
hapo. Lakini kama tukiendelea kukaa hapa, bado tutakufa. Sawa, njoni, twendeni
kwenye lile jeshi la Washami. Kama wakitupa uhai, tutakuwa hai, na kama wakituua,
tutakufa tu.” 5 Hivyo wakaamka asubuhi kabla giza halijaisha kwenda kwenye
kambi ya Washami; Wakati walipofika sehemu ya mwanzo wa kambi, hapakuwa
na mtu hapo. 6 Kwa kuwa Bwana alikuwa ameunda jeshi la Washami kusikia
sauti ya magari ya farasi, na sauti za farasi-sauti za jeshi jingine kubwa, ndipo
wakaambizana kila mmoja wao, “Yule mfalme wa Israeli amekodisha wafalme wa
Wahiti na Wamisri waje wapigane dhidi yetu.” 7 Hivyo wale maaskari wakaondoka
kungali giza; waliacha mahema yao, punda zao, na kambi kama ilivyokuwa, na
kukimbia kwa ajili ya maisha yao. 8 Wakati wale watu wenye ukoma walipokuja
sehemu ya mwisho wa kambi, wakaenda kwenye hema moja na kula na kunywa, na
kubeba fedha na dhahabu na nguo, na kwenda na kuzificha. Wakarudi na kuingia
kwenye hema nyingine na kubeba kutoka pale pia, na kwenda kuvificha. 9 Basi,
wakaambizana kila mmoja, “Hatufanyi sahihi. Siku hii ni siku ya habari njema,
lakini tunanyamaza kimya kuhusu hili. Kama tukisubiri mpaka kutakapopambazuka,
adhabu itakuwa juu yetu. Basi, njoni, twendeni na kuwaambia nyumba ya mfalme.”
10 Kwa hiyo wakaenda na kuwaita mabawabu wa mji. Wakawaambia, wakisema,
“Tumeenda kambi ya Washami, lakini hapakuwa na mtu pale, hakuna sauti ya
mtu yeyote, lakini kulikuwa na farasi wamefungwa, na punda wamefungwa, na zile
hema kama zilivyokuwa.” 11 Ndipo mabawabu wakatoa habari, ndipo wakaambiwa
ndani ya nyumba ya mfalme. 12 Basi yule mfalme akainuka usiku nakusema
kwa watumishi wake, “Nitawaambia sasa kile ambacho Washami walichotufanyia.
Wanajua kwamba tunanjaa, hivyo wameondoka kwenye kambi kwenda kujificha
kwenye mashamba. Wanasema, 'Wakati watakapotoka mjini, tutawakamata wakiwa
hai, na kuingia mjini.” 13 Mmoja wa wale watumishi wa mfalme akajibu na kusema,
“Nakuomba, ngoja baadhi ya watu wachukue farasi watano wale waliosalia, ambao
wamebaki kwenye mji. Wako kama mkutano wote wa Israeli waliobaki-wengi
wamekufa; ngoja tuwatume na tuone.” 14 Hivyo wakachukua magari mawili ya
farasi pamoja na farasi, na mfalme akawatuma baada ya jeshi la Washami, akisema,
“Enendeni mkaone.” 15 Wakawafuata kwenda Yordani, na barabara zote zilikuwa
zimejaa na vifaa ambavyo Washami walivitupa wapate kukimbia haraka. Kwa
hiyo wale wajumbe wakarudi na kumwambia mfalme. 16 Wale watu wakatoka
nje na wakaziteka nyara zile kambi za Washami. Hivyo kipimo cha unga mzuri
uliuzwa kwa shekeli moja, na vipimo viwili vya shayiri kwa shekeli moja, kama
vile ambavyo neno la Yahwe lilivyosema. 17 Naye mfalme alimwagiza yule nahodha
ambaye alitegemea mkono wake kuwa mkuu wa lango, na watu wakamkanyaga
chini langoni. Alikufa kama mtu wa Mungu alivyosema, ambaye ameongea wakati
yule mfalme alipomshukia. 18 Basi ikatokea kama yule mtu wa Mungu alivyosema
kwa mfalme akisema, “Mda kama huu kwenye lango la Samaria, vipimo viwili vya
shayiri vitapatikana kwa shekeli, na kipimo cha unga mzuri kwa shekeli.” 19 Yule

nahodha alimjibu yule mtu wa Mungu na kusema, “Tazama, hata kama Yahwe
angefanya madirisha mbinguni, je hiki kitu kingeweza kutokea” Elisha akasema,
“Tazama, utaona kikitokea kwa macho yako mwenyewe, lakini hutakula chochote
katika hicho.” 20 Hivyo ndivyo haswa kilichompata, kwa kuwa watu wakamkanyaga
kwenye lango, na kufa.

# 8

1 Basi, Elisha alikuwa amemwambia yule mwanamke ambaye alimfufulia mtoto
wake. Akamwambia, “Inuka na uenede pamoja na nyumba yako, na uishi popote
uwezapo katika nchi nyingine, kwa sababu Yahwe ameiita njaa ambayo itakuja katika
hii nchi kwa miaka saba.” 2 Basi yule mwanamke akainuka na akatii lile neno la
mtumishi wa Mungu. Akaenda na nyumba yake na kuishi kwenye nchi ya Wafilisti
miaka saba. 3 Ikafika kama mwishoni mwa miaka saba yule mwanamke akarudi
kutoka kwenye ile nchi ya Wafilisti, na kwenda kwa mfalme kumuomba nyumba
yake na kwa ajili ya nchi yake. 4 Basi mfalme alikuwa anaongea na Gehazi yule
mtumishi wa Mungu, akisema, “Tafadhali niambie yale mambo makubwa ambayo
Elisha ameyafanya.” 5 Basi alipokuwa akimwambia yule mfalme jinsi gani Elisha
alivyomfufua yule mtoto aliyekufa, huyo mwanamke ambaye mtoto wake aliyekuwa
amefufuliwa akaja kumuomba yule mfalme kwa ajili ya nyumba yake na nchi yake.
Gehazi akasema, “Bwana wangu, mfalme, huyu ndiye yule mwanamke, na huyu
ndiye mtoto wake, ambaye Elisha amemfufua.” 6 Wakati yule mfalme alipomuuliza
yule mwanamke kuhusu mtoto wake, alimwelezea yule mfalme. Ndipo mfalme
akamwagizia ofisa makini, akisema, “Mrudishie vyote vilivyokuwa vyake na mavuno
yake yote ya kwenye mashamba tangu siku alipoondoka hadi sasa.” 7 Elisha akaja
Damaskasi ambako Ben Hadadi yule mfalme wa Shamu alikuwa anaumwa. Yule
mfalme aliambiwa, “Yule mtu wa Mungu amekuja hapa.” 8 Mfalme akamwambia
Hazaeli, “Chukua zawadi kwenye mkono wako na uende ukakutane na mtu wa
Mungu, na ukazungumze na Yahwe kupitia yeye, ukisema, “Je nitapona huu ugonjwa
wangu?” 9 Basi Hazaeli akaenda kuonana naye na kuchukua zawadi zake za
kila kitu kizuri cha Damskasi, akabeba ngamia arobaini. Hivyo Hazaeli akaja na
kusimama mbele ya Elisha na kusema, “Mtoto wako Ben Hadadi mfalme wa Shamu
amenituma kwako, kusema, “Je nitapona huu ugonjwa?” 10 Elisha akamwambia,
“Nenda, kwa Ben Hadadi, 'Utapona hakika,' lakini Yahwe amenionyesha kwamba
atakufa hahkika.” 11 Basi Elisha akamtumbulia macho Hazaeli hadi alipojisikia
aibu, na yule mtu wa Mungu akalia machozi. 12 Hazaeli akauliza, kwa nini unalia,
bwana wangu?” Akajibu, “Kwa sababu najua uovu ambao utakaoufanya kwa watu
wa Israeli. Utazichoma moto ngome zao kwa moto, na utawaua vijana wao kwa
upanga, kuwaseta vipande vipande watoto wao wachanga, na kuwapasua mimba
zao wanawake wenye mimba.” 13 Hazaeli akajibu, Ni nani mtumwa wako, ambaye
atafanya jambo hili kubwa? Yeye ni mbwa tu.” Elisha akajibu, “Yahwe amenionyesha
kwamba utakuwa mfalme juu ya Shamu.” 14 Ndipo Hazaeli akamwacha Elisha na
kuja kwa bwana wake, ambaye alimwambia, “Je Elisha alikwambiaje?” Akajibu,
“Ameniambia kwamba utapona bila shaka.” 15 Basi siku ya pili yake Hazaeli
akachukua blangeti na kulichovya kwenye maji, na kulitandaza kwenye uso wa
Ben Hadadi hivyo akafa. Basi Hazaeli akawa mfalme katika sehemu sehemu yake.
16 Katika mwaka wa kumi na tano wa Yoramu mwana wa Ahabu, mfalme wa Israeli,
Yehoramu akaanza kutawala. Alikuwa mwana wa Yehoshafati mfalme wa Yuda.
Alianza wakati Yehoshafati alikuwa mfalme wa Yuda. 17 Yoramu alikuwa na umri
wa miaka thelathini na mbili alipoanza kutawala, na alitawala kwa mda wa miaka
minane katika Yerusalemu. 18 Yoramu akatembea kwenye njia ya huyo mfalme

wa Israeli, kama walivyokuwa wakifanya kwenye nyumba ya Ahabu; kwa kuwa alikuwa na binti wa Ahabu kama mke wake, na alifanya uovu usoni kwa Yahwe.
19 Walakini, kwa sababu ya mtumishi wake Daudi, Yahwe hakutaka kuiharibu Yuda, tangu alipomwambia kwamba atampatia wazao. 20 Katika siku za Yoramu, Edomu akaasi kutoka chini ya mkono wa Yuda, na wakamfanya mfalme juu yao wenyewe.
21 Basi Yehoramu akaenda na maamri jeshi na magari ya farasi yote. Ilitokea kwamba akaamka usiku na kushambulia na kuwazunguka Waedomu, waliokuwa wamemzunguka na wale maamri jeshi wa magari ya farasi. Ndipo wanajeshi wa Yehoramu wakakimbilia wajumbani kwao. 22 Hivyo Edomu aliasi dhidi ya utawala wa Yuda katika siku hizi. Libna pia aliasi katika kipindi hicho hicho. 23 Kwa mambo mengine yamhusuyo Yehoramu, yote aliyoyafanya, je hayakuandikwa kwenye kitabu cha matukio ya mfalme wa Yuda? 24 Yehoramu akafa na kuzikwa pamoja na baba zake, na akalala pamoja na baba zake katika mji wa Daudi. Ndipo Ahazi mtoto wake akawa mfalme katika sehemu yake. 25 Katika mwaka wa kumi na mbili wa Yohoramu mwana wa Ahabu, mfalme wa Israeli, Ahazi mwana wa Yehoramu, mfalme wa Yuda, alianza kutawala. 26 Ahazi alikuwa ana umri wa miaka ishirini na mbili wakati alipoanza kutawala; alitawala kwa mda wa mwaka mmoja katika Yerusalemu. Mama yake alikuwa anaitwa Athalia; alikuwa mtoto wa Omri, mfalme wa Israeli.
27 Ahazia alitembelea katika nyumba ya Ahabu; alifanya yale yaliyo maovu katika uso wa Yahwe, kama nyumba ya Ahabu ilivyokuwa ikifanya, kwa kuwa Ahazia alikuwa mkwe kwenye nyumba ya Aabu. 28 Ahazia akaenda pamoja na Yoramu mwana wa Ahabu, kupigana dhidi ya Hazaeli, mfalme wa Shamu, katika Ramath Geleadi. Washami wakamjeruhi Yoramu. 29 Mfalme Yoramu akarudi ili auguzwe huko Yezreeli kwenye yale majeraha ambayo Washami walimpatia huko Rama. Wakati alipopigana dhidi ya Hazaeli mfalme wa Shamu. Hivyo Ahazi mwana wa Yehoramu, mfalme Yuda, akashuka kwa Yezreeli kumuona Yoramu mwana wa Ahabu, kwa sababu Yoramu alikuwa amejeruhiwa.

# 9

1 Nabii Elisha akamwita mmoja wa watoto wa manabii na kumwambia, “Vaa kwa kwa safari, halafu chukua hii chupa ndogo ya mafuta kwenye mikono yako na uende Romoth Geliadi. 2 Wakati utakapofika, mtafute Yehu mwana wa Yehoshafati mwana wa Nimshi, na uende ukaingie na kumfanya ainuke kutoka miongoni mwa rafiki zake, na ukampeleke katika chumba cha ndani. 3 Kisha chukua ile chupa ya mafuta na imiminie kwenye kichwa chake na kusema, 'Yahwe anasema hivi: “Nimekumiminia mafuta uwe mfalme juu ya Israeli. “Halafu fungua mlango, na kukimbia; usichelewe.” 4 Basi yule kijana, yule nabii kijana, akaenda Romoth Geliadi.
5 Wakati alipofika, kumbe, wale manahodha wa lile jeshi walikuwa wamekaa. Hivyo yule nabii kijana akasema, “Nimekuja mara moja naneno kwako, nahodha.” Yehu akajibu, “kwa yupi katika sisi?” Yule nabii kijana akajibu, “Kwako nahodha.” 6 Basi Yehu akainuka na kwenda kwenye nyumba, na yule nabii akammiminia mafuta kwenye kichwa chake na kumwambia Yehu, “Yahwe, Mungu wa Israeli, anasema hivi: 'Nimekumiminia mafuta uwe mfalme juu ya watu wa Yahwe, juu ya Isaraeli.
7 Wewe lazima uiue familia ya Ahabu bwana wako, ili niweze kulipiza kisasi cha damu ya watumishi wangu manabii, na damu ya watumishi wote wa Yahwe, ambao waliokuwa wameuawa kwa mkono wa Yezebeli. 8 Kwa kuwa nyumba yote ya Ahabu itaangamia, na nitamkatilia mbali kila mtoto wa kiume wa Ahabu, yeyote awe mtumwa au mtu huru. 9 Nitaifanya nyumba ya Ahabu kama nyumba ya Yerobohamu mwana wa Nebati na kama nyumba ya Baasha mwana wa Ahiya. 10 Mbwa watamla Yezebeli katika Yezreeli, na hakutakuwa na mtu wa kumzika.” Kisha nabii akafungua

mlango na kukimbia. 11 Kisha Yehu akatoka kwenda kwa watumishi wa bwana wake,
na mmoja akamwambia, “Je kila kitu kiko sawa? Kwa nini huyu mwenda wazimu
amekuja kwako?” Yehu akawajibu, “Mnamjua huyo mtu na mambo asemayo.”
12 Wakasema, “Huo ni uongo. Tuambie.” Yehu akajibu, “Alisema hivi na vile juu
yangu, na pia akasema, 'hivi ndivyo Yahwe asemavyo: Nimekumiminia mafuta kama
mfalme juu ya Israeli.”” 13 Kisha kila mmoja wao akachukua vazi haraka na kuweka
chini ya Yehu juu ya madaraja. Wakapiga baragumu na kusema, “Yehu ni mfalme.”
14 Katika njia hii Yehu mwana wa Yehoshafati mwana wa Nimshi akafanya njama juu
ya Yoramu. Basi Yoramu alikuwa akiilinda Ramothi Gileadi, yeye na Israeli yote, kwa
sababu ya Hazaeli mfalme wa Shamu, 15 lakini mfalme Yoramu alikuwa amesharudi
kwa Yezreeli ili kuponywa yale majeraha aliyokuwa ameyapewa na Washami, wakati
akiwa anapigana dhidi ya Hazaeli mfalme wa Shamu. Yehu akawaambia watumishi
wa Yoramu, “kama hili ndilo wazo lako, kisha usimwache mtu aondoke na kwenda
nje ya mji, ili aende kupeleka habari hii Yezreeli.” 16 Basi Yehu akaendesha gari la
farasi mpaka Yezreeli; kwa kuwa Yoramu alikuwa amelala huko. Basi Ahazi mfalme
wa Yuda alikuwa ameshuka chini kuonana na Yoramu. 17 Mlinzi alikuwa amesimama
juu ya mnara katika Yezreeli, akaliona lile kundi la Yehu alipokuwa akija kwa mbali
kidogo; akasema, “Naona kundi la watu wanakuja.” Yoramu akasema, “Chukua
mwendesha farasi, na umtume akakutane nao; mwambie aseme, “Je mnakuja kwa
amani?”” 18 Hivyo mwendesha farasi akatoka kumlaki; akasema, “Mfalme asema
hivi: Je mnakuja kwa amani?”' Basi Yehu akasema, “Wewe una nini na amani?
Geuka na unifuate nyuma.” Kisha yule mlinzi akamwambia mfalme, Yule mjumbe
ameshaonana nao, lakini anarudi.” 19 Kisha akapeleka mpanda farasi wa pili, ambaye
alikuja kwao na kusema, “Mfalme asema hivi: 'Je mnakuja na amani?”' Yehu akajibu,
“Wewe una nini na amani? Geuka na kunifuata nyuma. 20 Tena yule mlinzi akatoa
taarifa, “Amekwisha kuonana nao, lakini hatorudi. Kwa kuwa hilo gari la farasi
limekuwa likiendeshwa ndivyo ambavyo Yehu mwana wa Nimshi aendeshavyo;
anaendesha kwa kasi.” 21 Hivyo Yoramu akasema, “Andaa gari langu la farasi liwe
tayari.” Wakaandaa gari lake la farasi, na Yoramu mfalme wa Israeli na Ahazi
mfalme wa Yuda akaendesha, kila mmoja kwenye gari lake la farasi, kumlaki Yehu.
Wakamkuta kwenye mali ya Nabothi Myezreeli. 22 Wakati Yoramu alipomuona Yehu,
alisema, “Je unakuja katika hali ya amani, Yehu?” Akajibu, “Amani gani hapo, wakati
uzinzi wa ukahaba hufanywa na uchawi wa mama yako Yezebeli umejaa tele?” 23 Basi
Yoramu akarudisha magari yake ya farasi na kukimbia na kumwambia Ahazia, “Kuna
udanganyifu, Ahazia. 24 Ndipo Yehu akauvuta upinde wake kwa nguvu zake zote
na kumpiga Yoramu kati ya mabega yake; mshale ukaenda kwenye moyo wake,
akaanguka chini kwenye gari lake la farasi. 25 Ndipo Yehu akamwambia Bidkari
nahodha wake, “Mchukue na mtupie kwenye shamba la Nabothi Myezreeni. Fikiria
kuhusu vile ambavyo wewe na mimi tulivyoendesha pamoja baada ya Ahabu baba
yake, Yahwe aliuweka juu unabii dhidi yake: 26 Jana niliona damu ya Nabothi na
damu ya watoto wake - asema Yahwe - na nitahakikisha unalipia hili shamba - asema
Yahwe. Sasa basi, mchukue na mtupe kwenye hili shamba, sawa sawa na neno
la Yahwe.” 27 Wakati Ahazi yule mfalme wa Yuda alipoliona hili, akakimbia kwa
njia ya Bethi Hagani. Lakini Yehu akamfuata, na kusema, “Muulie humo kwenye
gari la farasi,” na wakampiga mahali pa kupandia Guri, karibu na Ebleamu. Ahazi
akakimbilia Megido na kufia pale. 28 Watumishi wake wakaubeba mwili wake kwa
magari ya farasi kwenda Yerusalemu na kumzika kwenye kaburi lake pamoja na
baba zake katika mji wa Daudi. 29 Basi ilikuwa mwaka wa kumi na moja wa Yoramu
mwana wa Ahabu huyo Ahazia akaanza kutawala juu ya Yuda. 30 Wakati Yahu
alipokuja kwa Yezebeli, Yezebeli akasikia juu ya hilo, akapaka wanja kwenye macho

yake, akatengeneza nywele zake vizuri, na kuchungulia kwenye dirisha. 31 Kadiri
Yehu alipokuwa akiingia kwenye lango, akamwambia, “Je unakuja kwa amani, wewe
Zimri, muuaji wa bwana wako?” 32 Yehu akatazama juu ya dirisha na kusema, “Ni
nani yuko upande wangu? Nani?” Matowashi wawili au watatu wakachungulia nje.
33 Basi Yehu aksema, “Mtupeni chini.” Hivyo wakamtupa Yezebeli chini, na damu
yake nyingine ikamwagika kwenye ukuta na farasi, na Yehu akamkanyaga kanyaga
chini ya miguu. 34 Basi Yehu akaingia hiyo sehemu, akala na kunywa. Kisha akasema,
“Mtazamani sasa huyu mwanamke aliyelaaniwa na kumzika, kwa kuwa ni binti wa
mfalme.” 35 Wakaenda kumzika, lakini hawakumkuta ila fuvu, miguu, na viganga
vya mikono yake. 36 Basi wakarudi na kumwambia Yehu. Akasema, “Hili ndilo neno
la Yahwe ambalo ameliongea kupitia Eliya Mtishbi, likisema, 'Katika nchi Yezreeli
mbwa ataula mwili wa Yezebeli, 37 na mwili wa Yezebeli utakuwa kama kinyesi juu
ya uso wa mashamba katika nchi ya Yezreeli, kwa hiyo basi hakuna atakayeweza
kusema, “Huyu ni Yezebeli.””

# 10

1 Basi Ahabu alikuwa na watoto sabini katika Samaria. Yehu akaandika barua na
kuzituma kwenda Samaria, kwa watawala wa Yezreeli, pamoja na wazee na walinzi
wa wana wa Ahabu akisema, 2 “Wana wa bwana wako wako pamoja na wewe, na
wewe pia una magari ya farasi na farasi na kuimarisha mji dhidi ya maadui na silaha.
Hivyo basi, haraka iwezekanavyo barua hii ikufikiapo, 3 mchagueni aliye bora na
anayestahili miongoni mwa mtoto wa bwana wenu na kumuweka kwenye kiti cha
kifalme cha baba yake, na kupigania ufalme wa bwana wenu.” 4 Lakini waliogopa na
kusema miongoni mwao, “Tazama, wafalme wawili hawatasimama mbele ya Yehu.
Hivyo tutasimamaje?” 5 Kisha yule mtu ambaye alikuwa kiongozi kwenye nyumba ya
mfalme, na wale waliowalea watoto, wakatuma ujumbe kwa Yehu, kusema, “Sisi ni
watumishi wako. Tutafanya chochote utakacho tuamuru. Hatutamfanya mtu yeyote
kuwa mfalme. Fanya lile lililojema machoni pako.” 6 Kisha Yehu akaandika barua
mara ya pili, akisema, “Kama mko upande wangu, na kama mtasikiliza sauti yangu,
mtachukua vichwa vya watu wa wana wa mabwana wenu, na mje kwangu Yezreeli
kesho mda kama huu.” Ndipo wana wa wafalme, sabini kwa hesabu, waliokuwa
watu muhimu huko mjini, ambao walikuwa wakiwaleta. 7 Hivyo barua ilipokuja
kwao, waliwachukua wana wa wafalme na kisha kuwaua, watu sabini, wakaweka
vichwa vyao kwenye vikapu, na kuivituma kwa Yehu katika Yezreeli. 8 Mjumbe
mmoja akaja kwa Yehu, akisema, “Wamevileta vile vichwa vya watoto wa wafalme.”
Hivyo akasema, viwekeni kwenye mafungu mawili kwenye lango hadi asubuhi.”
9 Asubuhi Yehu akatoka nje na kusimama, na kusema kwa watu wote, “Ninyi hamna
hatia. Tazameni, nimefanya fitina dhidi ya bwana wangu na kumuua, lakini ni nani
aliyewaua hawa wote? 10 Sasa hakika tafakarini kwamba hakuna sehemu ya neno
la Yahwe, lile alilonena Yahwe kuhusu familia ya Ahabu, itaanguka kwenye aridhini,
kwa kuwa Yahwe amefanya kile alichokiongea kupitia mtumishi wake Eliya.” 11 Basi
Yehu akawaua wote waliokuwa wamebakia wa familia ya Ahabu katika Yezreeli, na
watu wake muhimu wote, marafiki zake wa karibu, na makuhani wake, hakuna hata
mmoja wao alisalia. 12 Kisha Yehu akainuka na kuondoka; akaenda Samaria. Kadiri
alivyokuwa akikaribia Bethi Ekedi ya wachungaji, 13 akamlaki na ndugu wa Ahazia
mfalme wa Yuda. Yehu akawaambia, “Ninyi ni akina nani?” Wakajibu, “Sisi ni ndugu
zake na Ahazia, na tunashuka chini kuwasalimia watoto wa mfalme na watoto wa
Malkia Yezebeli.” 14 Yehu akawaambia watu wake mwenyewe, “Wachukue wakiwa
hai.” Hivyo wakawachukua wakiwa hai na kuwaua kwenye kisima cha Bethi Ekedi,
watu wote arobaini na mbili. Hakumwacha hata mmoja wao akiwa hai. 15 Baada

ya Yehu kuondoka huko, akakutana na Yehonadabu mwana wa Rekabu anakuja
kukutana naye. Yehu akamsalimia na kisha akamwambia, “Je moyo wako uko na
mimi, kama moyo wangu ulivyo pamoja na wako?” Yehonadabu akajibu, Ndio.”
Yehu akasema, “kama ni ndio, nipatie mkono wako.” Kisha Yehonadabu akampatia
mkono wake, na Yehu akampandisha Yehonadabu juu kwenye magari ya farasi
pamoja naye. 16 Yehu akasema, “Fuatana pamoja nami na uone wivu wangu kwa
Yahwe.” Hivyo alikuwa na Yehonadabu akiendesha gari la farasi. 17 Wakati alipokuja
Samaria, Yehu akawaua wote waliobakia kutoka uzao wa Ahabu katika Samaria,
hata akawaangamiza ukoo wa kifalme wa Ahabu, kama walivyokuwa wameambiwa
kabla ya neno la Yahwe, ambalo aliloambiwa Eliya. 18 Kisha Yehu akawakusanya
watu wote akwaambia, “Ahabu alimtumikia Baali kidogo, lakini Yehu atamtumikia
sana. 19 Basi niitieni manabii wote wa Baali, wote wamwabuduo, na makuhani wake
wote. Asikosekane mtu hata mmoja, kwa kuwa nina dhabihu kubwa nataka kutoa
kwa Baali. Yeyote atakayeshindwa kuja hataishi.” Lakini Yehu alifanya haya kwa
udanganyifu, kwa dhamira ya kuwaua wanaomwabudu Baali. 20 Yehu akasema,
“Tengeni mda tuwe na mkutano kwa ajili ya Baali.” Hivyo wakalitangaza. 21 Kisha
Yehu akatuma Israeli yote na wamwabuduo Baali waje, hivyo basi hakuna mtu hata
mmoja ambaye aliacha kuja. Walikuja kwenye hekalu la Baali, na ilijaa kutoka
mwanzo hadi mwisho. 22 Yehu akamwambia yule mtu aliyekuwa anatunza kabati
la nguo za makuhani, “Uwatolee mavazi wote wamwabuduo Baali.” Basi yule mtu
akawatolea nguo. 23 Basi Yehu akaingia pamoja na Yohonadabu mwana wa Rekabu
kwenye nyumba ya Baali, na kisha akawaambia wanaomwabudu Baali, “Tafuteni
na muhahakishe kwamba hakuna mtu hapa pamoja na ninyi kutoka watumishi wa
Yahwe, lakini wamwabuduo Baali peke yao.” 24 Kisha wakaenda kutoa dhabihu
na sadaka ya kutekeza. Basi Yehu alichagua watu themanini ambao walikuwa
wamesimama nje, na aliwaambia, Kama mtu yeyote miongoni mwa hawa watu
ambao nimewaleta kwenye mikono yenu atoroke, yeyote atakayemwacha huyo mtu
atoroke, maisha yake yatachukuliwa kwa ajili ya yule aliyeokoka.” 25 Hivyo kisha
baada ya mda mfupi Yehu alipomaliza kutoa sadaka ya kutekezwa, akamwambia
mlinzi na manahodha, “Ingieni na muwaue. Msimwache mtu yeyote atoke.” Basi
waliwaua kwa makali ya upanga, na mlinzi na manahodha wakawatupa nje na
kwenda kwenye chumba cha ndani cha nyumba ya Baali. 26 Wakazitoa nguzo za
mawe ambazo zilikuwa kwenye nyumba ya Baali, na kisha kuzichoma. 27 Kisha
wakazivunja zile nguzo za Baali, na kuiharibu nyumba ya Baali na kuifanya choo,
ambacho kipo hadi leo. 28 Hivi ndivyo ambavyo Yehu alivyomharibu muabudu Baali
kutoka Israeli. 29 Lakini Yehu hakuacha dhambi za Yeroboamu mwana wa Nebati,
ambayo ilfanya Israeli kutenda dhambi-ambayo ni, kumwabudu ndama wa dhahabu
katika Betheli na Dani. 30 Hivyo Yahwe akamwambia Yehu, “Kwa kuwa umefanya
vema kwa kufanya yaliyo sahihi kwenye macho yangu, na kumailiza kwenye nyumba
ya Ahabu kulingana na yote yaliyokuwa kwenye moyo wangu, uzao wako utakaa
kwenye kiti cha Israeli hadi kizazi cha nne.” 31 Lakini Yehu hakujali kutembea
kwenye sheria ya Yahwe, Mungu wa Israeli, kwa moyo wake wote. Hakugeuka
kutoka kwenye dhambi za Yeroboamu, ambayo iliwafanya Israeli kutende dhambi.
32 Siku zile Yahwe akaanza kupunguza mikoa ya Israeli, na Hazaeli kuwashinda
Waisraeli mipakani mwa Israeli, 33 kutoka Yordani upande wa mashariki, nchi yote ya
Gileadi, Wagadi, na Wareubeni, na Wamanase, kutoka Aroeri, alipo karibu na bonde
la Arnoni, kupita Geleadi hadi Bashani. 34 Kama kwa mambo mengine yamhusuyo
Yehu, na yote aliyoyafanya, na ushujaa wake, je hayakuandikwa kwenye kitabu cha
matukio ya wafalme wa Israeli? 35 Yehu akalala na wazee wake, na walimzika katika
Samaria. Kisha Yehoahazi mwanaye akawa mfalme katika sehemu yake. 36 Mda

ambao Yehu alitawala juu ya Israeli katika Samaria ulikuwa miaka ishini na nane.

## 11

1 Basi Athalia, mama yake na Ahazia, alipoona kwamba mtoto wake amekufa,
aliinuka na kuwaua watoto wote wa kifalme. 2 Lakini Yehosheba, binti wa mfalme
Yehoramu na dada wa Ahazia, akamchukua Yoashi mwana wa Ahazia, na kumficha
mbali mwa miongoni mwa watoto wa mfalme waliokuwa wameuawa, wakati wote
pamoja na mlezi wake; akawaweka kwenye chumba cha kulala. Wakamficha kutoka
Athalia kwa hiyo hakuuawa. 3 Alikuwa pamoja na Yehosheba, wamejificha kwenye
nyumba ya Yahwe, kwa mda wa miaka sita, wakati Athalia alipotawala juu ya
nchi. 4 Katika mwaka wa saba, Yehoyada alituma ujumbe na kuleta maamiri jeshi
mamia wa Wakari na wa walinzi, na kuwaleta kwake mwenyewe, ndani ya nyumba
ya Yahwe. Akafanya agano pamoja nao, na kuwaapisha kiapo katika nyumba ya
Yahwe. Kisha akawaonyesha mtoto wa mfalme. 5 Akawaamuru, akisema, “Hivi
ndivyo mnavyotakiwa kufanya. Theluthi yenu mtakaokuja kwenye Sabato mtakuwa
mkiiangalia nyumba ya mfalme, 6 na theluthi mtakuwa langoni mwa Suri, na theluthi
langoni nyuma ya walinzi.” 7 Makundi mengine mawili ambayo hayatumikii Sabato,
Mtayalinda juu ya nyumba ya Yahwe kwa ajili ya mfalme. 8 Ni lazima mumzunguke
mfalme, kila mmoja na silaha zake kwenye mkono wake. Yeyote aingiaye ndani
ya safu, auwawe. Lazima mkae pamoja na mfalme kila atokapo na kila aingiapo.
9 Hivyo mamia ya maamri jeshi wakatii kila kitu Yehoyada kuhani alichokiamuru.
Kila mmoja akachukua watu wake, wale ambao walitakiwa kuja kutumika siku
ya hiyo Sabato, na wale ambao wataacha kuitumika kwenye hiyo Sabato; ndipo
wakaja kwa Yehoyada kuhani. 10 Kisha Yehoyada yule kuhani akawapa mikuki
na ngao mamia wa maamri jeshi ambayo ilikuwa mali ya mfalme Daudi ambayo
ilikuwa kwenye nyumba ya Yahwe. 11 Basi walinzi wakasimama, kila mtu na silaha
kwenye mkono wake, kutoka upande wa kuume wa hekalu, kwenda upande wa
kushoto, karibu na madhabahu ya hekelu, wakimzunguka mfalme. 12 Kisha Yehoyada
akamleta nje mtoto wa mfalme Yoashi, na kumvalisha taji la kifalme, na kumpatia
mikataba ya agano. Kisha wakamfanya mfalme na kummiminia mafuta. Wakapiga
makofi wakisema, “Mfalme na aishi!” 13 Wakati Athalia aliposikia sauti za walinzi
na za watu, alikuja kwa wale watu kwenye nyumba ya Yahwe. 14 Akatazama, na,
kisha, yule mfalme alikuwa amesimama kwenye nguzo, kama ilivyokuwa desturi,
na manahodha na wapiga mabaragumu walikuwa karibu na mfalme. Watu wote
wa nchi hiyo walikuwa wakifurahi na kupiga matarumbeta. Kisha Athalia akachana
mavazi yake kwa hasira na kupiga kelele, “Uhaini! Uhaini!” 15 Ndipo Yehoyada yule
kuhani akawaagiza maamri jeshi wa mamia ambao waliokuwa juu ya jeshi, akisema,
“Mtoeni kwenye safu.” Atakayemfuata, muueni kwa upanga.” Kwa kuwa kuhani
alisema, “Msimwache auawe kwenye nyumba ya Yahwe.” 16 Hivyo wakamtwaa
kadiri walivyokuwa wakiikaribia hiyo sehemu iliyokuwa na farasi wakaingia chini,
na akauawa huko. 17 Kisha Yehoyada akafanya agano kati ya Yahwe na mfalme
na watu, ambao wangekuwa watu wa Yahwe, na pia kati ya mfalme na watu.
18 Basi watu wote wa nchi wakaenda kwenye nyumba ya Baali na kuingusha chini.
Wakaangusha madhabahu ya Baali na sanamu zake wakazivunja vipande vipande,
na kumuua Matani, mfalme wa Baali, mbele ya haya madhabahu. Kisha Yehoyada
kuhani akawachagua walinzi juu ya hekalu la Yahwe. 19 Yehoyada akawachukua
maamiri jeshi wa mamia, Wakari, walinzi, na watu wote wa nchi, na kwa pamoja
wakamleta chini mfalme kutoka kwenye nyumba ya Yahwe na wakaenda kwenye
nyumba ya mfalme, wakaingia kwa njia ya lango la walinzi. Yoashi akachukua nafasi
yake kwenye kiti cha enzi cha mfalme. 20 Hivyo watu wote wa nchi wakamsifu,

na nchi ilikuwa kimya baada ya Athalia kuuawa kwa upanga kwenye nyumba ya
mfalme. 21 Yoashi alikuwa na umri wa miaka saba tangu alipoanza kutawala.

# 12

1 Katika mwaka wa saba wa Yehu, utawala wa Yoashi ulianza; alitawala kwa
mda wa miaka arobaini huko Yerusalimu. Mama yake alikuwa anaitwa Sibia, wa
Beersheba. 2 Yoashi akafanya yaliyo mema usoni mwa Yahwe siku zote, kwa sababu
Yehoyada kuhani alimfundisha. 3 Lakini sehemu ya juu haikuchukuliwa. Watu
wakaendelea kutoa sadaka na kuchoma ubani kwenye sehemu za juu. 4 Yoashi
akamwambia kuhani, "Pesa zote zilizokuja kama sadaka takatifu kwenye nyumba
ya Yahwe, pesa ya matumizi pesa ya watu kadiri alivyoandikiwa kila mtu, na
pesa yote aonayo moyoni mwake kuileta kwenye nyumba ya Yahwe- 5 makuhani
watapokea pesa kutoka miongoni mwa mmoja wa watunza pesa na kutengeneza
kila sehemu itakayoonekana imeharibika kwenye hekalu." 6 Lakini kama mwaka
wa ishirini na tatu wa mfalme Yoashi, makuhani hawakuwa wameandaa kitu
chochote kwenye hekalu. 7 Mfalme Yoashi akamwita Yehoyada kuhani na kuhani
mwingine; akawaambia, "Kwa nini hamjaandaa kitu chochote kwenye hekalu? Sasa
msichukue tena pesa kutoka kwa walipa kodi wenu, lakini chukueni kile kilichokuwa
kikikusanywa kwa ajili ya matengenezo ya hekalu na uwapatia wale wanaoweza
kufanya matengenezo. 8 Hivyo makuhani wakakubaliana wasichukue pesa tena
kutoka kwa watu na wasitengeneze wenyewe. 9 Badala yake, Yehoyada yule kuhani
akachukua kasha, akatoboa tundu kwenye kifuniko chake, na kuliweka karibu na
madhabahu, upande wa kulia kama mtu anaingia kwenye madhabahu ya Yahwe.
Makuhani ambao walikuwa wakilinda mlango wa hekalu wakatumbukiza pesa zote
ambazo zilizokuwa zimeletwa kwenye nyumba ya Yahwe. 10 Ikawa walipoona
kwamba kulikuwa na pesa za kutosha kwenye kasha, mwadishi wa mfalme na kuhani
mkuu wakaja na kuweka pesa kwenye mifuko na kisha kuhesabu, pesa ikaonekana
kwenye nyumba ya Yahwe. 11 Wakawapa pesa ambayo ilikuwa imepimwa kwenye
mikono ya watu ambao waliokuwa wanatunza nyumba ya Yahwe. Wakawalipa
mafundi seremala na wajenzi ambao walikuwa wemefanya kazi kwenye nyumba ya
Yahwe, 12 na waashi na wakata mawe, kwa ajili ya kununua mbao na kukata mawe
kwa ajili ya kutengenezea nyumba ya Yahwe, na yote iliyokuwa inahitajika kulipwa
kwa ajili ya kuitengeneza. 13 Lakini ile pesa iliyokuwa imeletwa kwenye nyumba
ya Yahwe haikulipwa kwa ajili ya vikombe vya fedha, mabeseni, au dhahabu au
fedha yoyote ya vyombo. 14 Waliwapa hizi fedha wale ambao waliokuwa wamefanya
kazi ya kutengeneza nyumba ya Yahwe. 15 Pia, hakukuhitajika zile pesa zilipwe
kwa ajili ya matengenezo ili kuwajibika kwa kuwa watu walizipokea nakuzilipa
kwa watenda kazi, kwa sababu hawa watu walikuwa waadilifu. 16 Lakini pesa
kwa ajili ya matoleo ya hatia na pesa kwa ajili ya matoleo ya dhambi hazikuwa
zimeletwa kwenye hekalu la Yahwe, kwa sababu zilikuwa mali ya makuhani.
17 Kisha Hazaeli mfalme wa Shamu akashambuliwa na kupigana dhidi ya Gathi, na
kuichukua. 18 Ndipo Hazaeli akageuka kuishambulia Yerusalemu. Yoashi mfalme
wa Yuda akavichukua vitu vyote ambavyo Yehoshefati na Yehoramu na Ahazia,
baba zake, wafalme wa Yuda, na kuviweka wakfu, na vile alivyokuwa ameviweka
wakfu, na dhahabu zote zilizokuwa zimeonekana kwenye gala la nyumba ya Yahwe
na la mfalme akawatuma kwenda kwa Ahazi mfalme wa Shamu. Kisha Hazaeli
akaenda zake kutoka Yerusamu. 19 Kama mambo mengine yanayomuhusu Yoashi,
yote aliyoyafanya, je hayakuandikwa kwenye kitabu cha matukio ya wafalme wa
Yuda? 20 Watumishi wake wakainuka na kupanga pamoja; wakamteka Yoashi katika
Bethi Milo, kwenye njia ya kushukia kwa Sila. 21 Yozakari mwana wa Shimeathi,

na Yehozabadi mwana wa Shomeri, watumishi wake, wakamshambulia na akafa. Wakamzika Yoashi pamoja na mababu zake katika mji wa Daudi, na Amazia, mtoto wake, akawa mfalme kwenye sehemu yake.

# 13

1 Katika mwaka wa ishirini na tatu wa Yoashi mwana wa Ahazia mfalme wa Yuda,
Yehoazi mwana wa Yehu alianza kutawala juu ya Israeli katika Samaria; alitawala
miaka kumi na saba. 2 Alifanya yaliyo maovu usoni mwa Yahwe na kufuata dhambi
za Yeroboamu mwana wa Nebati, ambaye alisababisha Israeli kuasi; na Yehoazi
hakurudi kutoka kwao 3 Hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli, na akaendelea
kuwakabidhi kwenye mikono ya Hazaeli mfalme wa Shamu na kwenye mikono
ya Ben Hadadi mwana wa Hazaeli. 4 Hivyo Yehoazi akamsihi Yahwe, na Yahwe
akamsikiliza kwa sababu aliona mateso ya Israeli, vile mfalme wa Shamu alivyokuwa
akiwatesa. 5 Basi Yahwe akawapa Israeli ulinzi, na wakakimbia kutoka kwenye
mikono ya Washami, na watu wa Israeli wakaanza kuishi kwenye nyumba zao kama
walivyokuwa kabla. 6 Hata hivyo, hawakuziacha dhambi za nyumba ya Yeroboamu,
ambaye alisabisha Israeli kuasi, na wakaendelea katika hayo; na huyo Ashera akabaki
hivyo katika Samaria. 7 Washami wakamuacha Yehoazi pamoja na waendesha farasi
hamsini tu, magari ya farasi kumi, na watembea kwa miguu elfu kumi, kwa ajili ya
mfalme wa Shamu alikuwa ameiharibu na kuwafanya kama makapi yaliyopurwa.
8 Kama mambo mengine yanayomuhusu Yehoazi, na yote aliyoyafanya na nguvu
zake, je hayakuandikwa kwenye kitabu cha matukio ya wafalme wa Israeli? 9 Basi
Yehoyazi akalala na mababu zake, na wakamzika katika samaria. Yohoashi mwanaye
akawa mfalme katika sehemu yake. 10 Katika mwaka wa thelathini na saba wa Yoashi
mfalme wa Yuda, utawala wa Yehoashi mwana wa Yehoazi ulianza juu ya Israeli
katika Samaria; alitawala miaka kumi na sita. 11 Akafanya yaliyo maovu kwenye uso
wa Yahwe. Hakuacha nyuma dhambi zozote za Yeroboamu mwana wa Nebati, kwa
kuwa aliwafanya Israeli kuasi, lakini alitembea pamoja nao. 12 Kama kwa mambo
mengine yanayomuhusu Yehoashi, na yote aliyoyafanya, na shujaa wake ambaye
aliyepigana dhidi ya Amazia mfalme wa Yuda, je hayakuandikwa kwenye kitabu cha
matukio ya wafalme wa Israeli? 13 Yehoashi akalala na mababu zake, na Yeroboamu
akakalia kiti chake cha enzi cha kifalme. Yehoashi akazikwa katika Samaria pamoja
na wafalme wa Israeli. 14 Basi Elisha akaugua ugonjwa ambao baadae ulimuua,
hivyo Yehoashi yule mfalme wa Israeli akashuka chini kwake na kumlilia juu yake.
Akasema, “Baba yangu, baba yangu, haya magari ya farasi ya Israeli na hawa
waendesha farasi wanakuchukua!” 15 Elisha akamwambia, “Chukua upinde na
mishale,” basi Yoashi akachukua upinde na mishale. 16 Elisha akamwambia mfalme
wa Israeli, “Weka mkono wako kwenye upinde,” basi akaweka mkono wake kwenye
huo. Kisha Elisha akalaza mikono yake kwenye mikono ya mfalme. 17 Elisha akasema,
“Fungua dirisha upande wa mashariki,” basi akalifungua. Kisha Elisha akasema,
“Funga”, na akafunga. Elisha akasema, “Huu ndiyo mshale wa ushindi wa Yahwe,
huu mshale wa ushindi juu ya Shamu, kwa kuwa utawapiga Washami katika Afeki
hadi utakapowaangamiza.” 18 Kisha Elisha aksema, “Chukua mishale,” basi Yoashi
akaichukua. Akamwambia mfalme wa Israeli, “Piga chini pamoja nao,” na akapiga
chini mara tatu, kisha akaacha. 19 Lakini mtu wa Mungu alikuwa na hasira naye na
akasema, “Ungelipiga chini mara tano au mara sita. Ndipo ungeipiga Shamu hadi
kuiangamiza, lakini sasa utaipiga Shamu mara tatu tu.” 20 Kisha Elisha akafa, na
wakamzika. Sasa vikundi vya Wamoabi wakaingia kwenye nchi mwanzoni mwa
mwaka. 21 Ikawa walipokuwa wakimzika huyo mtu, wakaona kundi la Wamoabi,
hivyo wakautupia ule mwili kwenye kaburi la Elisha. Mara yule mtu alipoigusa

mifupa ya Elisha, alifufuka na kusimama kwa miguu yake. 22 Hazaeli mfalme
wa Shamu akawatesa Israeli siku zote za Yehoazi. 23 Lakini Yahwe aliwahurumia
Israeli, na alikuwa na huruma juu yao na kushuhulika kwa ajili yao, kwa sababu
ya agano lake na Ibrahimu, Isaka, na Yakobo. Hivyo Yahwe hakuwaangamiza, na
bado hakuwatupa kutoka kwenye uwepo wake. 24 Hazaeli mfalme wa Shamu akafa,
na Ben Hadadi mtoto wake akawa mfalme katika sehemu yake. 25 Yehoashi mwana
wa Yehoazi akairudisha kutoka kwa Ben Hadadi mwana wa Hazaeli miji ambayo
aliichukua kutoka Yehoazi baba yake kwa vita. Yehoashi akamshambulia mara tatu,
na akaipata miji ya Israeli.

# 14

1 Katika mwaka wa pili wa Yehoashi mwana wa Yehoazi, mfalme wa Israeli, Amazia
mwana wa Yoashi, mfalme wa Yuda, alianza kutawala. 2 Alikuwa na umri wa
miaka ishirini na tanao wakati alipoanza kutawala; alitawala kwa mda wa miaka
ishirini na tisa katika Yerusalemu. 3 Mama yake alikuwa anaitwa Yehoyadani, wa
Yerusalemu. Alifanya yale yaliyo mema usoni mwa macho ya Yahwe, sio kama baba
yake Daudi. Alifanya kila kitu ambacho Yoashi, baba yake, alichukuwa amekifanya.
4 Lakini sehemu ya juu haikuondolewa. Watu wakaendelea kutoa dhabihu na
kufukiza ubani katika sehemu mahala pa juu. 5 Ikawa mara utawala wake ulipokuwa
imara, aliwaua watumishi ambao waliokuwa wamemuua baba yake, mfalme. 6 Ila
hakuwaweka watoto wa wale wauaji kwenye kifo; isipokuwa, alifanya kutokana
na kile kilichokuwa kimeandikwa kwenye sheria, kwenye kitabu cha Musa, kama
Yahwe alivyokuwa ameamuru, akisema, "Wababa wasife kwa ajili ya watoto wao,
wala watoto wasife kwa ajili ya makosa ya wazazi wao. Isipokuwa, kila mtu atakufa
kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe." 7 Aliua maaskari elfu kumi wa Edomi
kwenye bonde la chumvi; pia alimchukua Sela kwenye vita na kuiita Yoktheeli,
ndivyo paitwavyo hadi leo. 8 Kisha Amazia akatuma wajumbe kwa Yehoashi
mwana wa Yehoahazi mwana wa Yehu mfalme wa Israeli, akisema, "Njoo, tuonane
kila mmoja macho kwa macho kwenye mashinadano." 9 Lakini Yehoashi mfalme
wa Israeli akawatuma wajumbe kurudi kwa Amazia mfalme wa Yuda, akisema,
"Mbaruti uliokuwa Lebanoni ulituma kwa mwerezi katika Lebanuni, kusema, 'Mpatie
mwanangu binti yako amuoe; lakini hayawani aliyekuwako Lebanoni akaukanyaga
chini ule mbaruti. 10 Umempiga sana Edomu, na moyo wako umekuinua. Jisifu
katika ushindi wako, lakini kaa nyumbani, kwa nini unataka kujisababishia mataizo
na kuanguka, wote wewe na Yuda pamoja nawe?" 11 Lakini Amazia hakutaka
kusikia. Hivyo Yehoashi mfalme wa Israeli akakwea yeye na Amazia mfalme wa
Yuda wakakutana uso kwa uso huko Beth Shemeshi, ambayo ilikuwa ya Yuda. 12 Yuda
walishindwa mbele ya Israeli, na kila mtu akakimbia nyumbani. 13 Yehoashi mfalme
wa Israeli, akamchukua Amazia, mfalme wa Yuda mwana wa Yehoashi mwana wa
Ahazia, huko Beth Shemeshi. Akaja Yerusalemu na kuuangusha chini ukuta wa
Yerusalemu kutoka lango la Efraimu mpaka kwenye pembe ya lango, urefu wa mbali
wa dhiraa mia nne. 14 Akachukua dhahabu na fedha zote, na vitu vyote ambavyo
vilipatikana katika nyumba ya Yahwe, na vitu vya thamani kwenye nyumba ya
mfalme, pamoja na mateka pia, na kurudi samaria. 15 Kama ilivyo kwa mambo
mengine yamhusuyo Yehoashi, yote aliyoyafanya, ushujaa wake, na jinsi alivyopigana
na Amazia mfalme wa Yuda, je hayakuandikwa kwenye kitabu cha matukio ya
mfalme wa Israeli? 16 Kisha Yehoashi akalala na wazee wake na ailizikwa katika
Samaria pamoja na wafalme wa Israeli, na Yeroboamu, mwanaye, akawa mfalme
katika eneo lake. 17 Amazia mwana wa Yoashi, mfalme wa Yuda, akaishi miaka
kumi na tano baada ya Yehoashi mwana wa Yehoahazi, mfalme wa Israeli. 18 Kama
ilivyo kwa mambo mengine yanayomhusu Amazia, je hayakuandikwa kwenye kitabu

cha matukio ya mfalme wa Yuda? [19] Wakafanya njama dhidi ya Amazia katika
Yerusalimu, akakimbilia Lakishi. Akakimbia hadi Lakishi, lakini wakawatuma watu
kumfuata hadi Lakishi na kumuua huko. [20] Wakamrudisha kwa farasi, na alizikwa
pamoja na wazee wake katika mji wa Saudi. [21] Watu wote wa Yuda wakamchukua
Uzaria, ambaye alikuwa na umri wa miaka kumi na minne, na walimfanya kuwa
mfalme katika nyumba ya kifalme wa baba yake Uzaria. [22] Alikuwa Uzaria ambaye
alijenga Elathi na kuirudisha kwa Yuda, baada ya mfalme Uzaria akalala pamoja
na mababu zake. [23] Katika mwaka wa kumi na tano wa Amazia mwana wa Yoashi
mfalme wa Yuda, Yeroboamu mwana wa Yoashi mfalme wa Israeli alianza kutawala
katika Samaria; alitawala kwa muda wa miaka arobaini na moja. [24] Akafanya yaliyo
maovu usoni mwa Yahwe. Hakuziacha dhambi zake za Yeroboamu mwana wa
Nabeti, ambaye aliisababisha Israeli kuasi. [25] Akairudisha mipaka ya Israeli kutoka
Lebo Hamathi mpaka kwenye Bahari ya Araba, kufuata amri ya neno la Yahwe,
Mungu wa Israeli, ambalo aliongea kupitia mtumishi wake Yona mwana wa Amitai,
yule nabii, ambaye alitokea Gathi Heferi. [26] Kwa kuwa Yahwe aliyaona mateso ya
Israeli, ambayo yalikuwa makali kwa kila mmoja, wote mtumwa na asyemtumwa,
na kwamba hapakuwa na ulinzi kwa ajili ya Israeli. [27] Basi Yahwe akasema kwamba
hatoweza kulifuta jina la Israeli chini ya mbingu; badala yake, aliwaokoa kwa mkono
wa Yeroboamu mwana wa Yehoashi. [28] Kama ilivyo kwa mambo mengine yamhusuyo
Yeroboamu, yote aliyoyafanya, ushujaa wake, jinsi alivyo pigana vita na kuipata tena
Damaskasi na Hamathi, ambayo ilikuwa ya Yuda, kwa Israeli, je hayakuandikwa
katika kitabu cha matukio ya wafalme wa Israeli? [29] Yeroboamu akalala na mababu
zake, pamoja na mfalme wa Israeli, na Zekaria mtoto wake akawa mfalme katika
sehemu yake.

# 15

[1] Katika mwaka wa ishirini na saba wa Yeroboamu mfalme wa Israeli, Azaria
mwana wa Amazia mfalme wa Yuda akaanza kutawala. [2] Azaria alikuwa na umri
wa miaka kumi na sita alipoanza kutawala, na alitawala kwa mda wa miaka
hamsini na mbili katika Yerusalemu. Mama yake alikuwa anaitwa Yekolia, na
alikuwa anatokea Yerusalemu. [3] Alifanya yaliyo mema machoni pa Yahwe, kama
baba yake Amazia alivyofanya. [4] Lakini, mahali pa juu hapakuwa pameondolewa.
Watu wakaendelea kutoa sadaka na kufukiza ubani katika mahala pa juu. [5] Yhawe
akampiga mfalme hivyo basi akawa na ukoma mpaka siku ya kifo chake na alikaa
kwenye nyumba ya pekee. Yothamu, mtoto wa mfalme, alikuwa juu ya watu na
kuwaongoza watu wa nchi. [6] Kama kwa mambo mengine yanayomhusu Azaria,
yote aliyoyafanya, je hayajaandikwa kwenye kitabu cha matukio ya wafalme wa
Yuda? [7] Hivyo Azaria alilala pamoja na babu zake katika mji wa Daudi. Yothamu,
mtoto wake, akawa mfalme katika mahala pake. [8] Katika mwaka wa thelathini na
nane mwaka wa Azaria mfalme wa Yuda, Zekaria mwana wa Yeroboamu akatawala
juu ya Israeli katika Samaria kwa miezi sita. [9] Alifanya yaliyo maovu usoni
mwa Yahwe, kama baba zake waliyoyafanya. Hakuziacha dhambi za Yeroboamu
mwana wa Nabeti, ambaye alisababisha Israeli kuasi [10] Shalumu mwana wa Yabeshi
akafanya njama dhidi ya Zekaria, akamshambulia katika Ibleamu, na kumuua. Kisha
akawa mfalme katika mahala pake. [11] Kama kwa mambo mengine yanayomuhusu
Zekaria, yameandikwa kwenye kitabu cha matukio ya wafalme wa Israeli. [12] Hili
ndilo lililokuwa neno la Yahwe ambalo aliongea na Yehu, kusema, "Kizazi chako
kitakaa katika kiti cha Israeli mpaka kizazi cha nne." Hiyo ikatokea. [13] Shalumu
mwana wa Yabeshi akaanza kutawala katika mwaka wa thelathini na tisa wa Azaria
mfalme wa Yuda, na kutawala kwa mwezi mmoja tu katika Samaria. [14] Menahemu
mwana wa Gadi akapanda kutoka Tirza kwenda Samaria. Akamshambulia Shalumu

mwana wa Yabeshi hapo, katika Samria. Akamuua na kuwa mfalme katika mahali
pake. 15 Kama kwa mambo mengine yanayomuhusu Shalumu na njama aliyoifanya,
yameandikwa kwenye kitabu cha matukio cha wafle wa Israeli. 16 Ndipo Menahemu
akamshambulia Tifsa na wote waliokuwa pale, na mipaka yote kuzunguka Tizra,
kwasababu hawakufungua kwenye mji. Hivyo akaushambulia, na akawapasua
wanawake wajawazito wote katika hicho kijiji. 17 Katika mwaka wa thelathini na
tisa wa Ahazia mfalme wa Yuda, Menahemu mwana wa Gadi akaanza kutawala;
alitawala kwa miaka kumi katika Samaria. 18 Alifanya yaliyo maovu usoni mwa
Yahwe. Katika maisha yake yote, hakuziacha dhambi za Yeroboamu mwana wa
Nabeti, ambaye alifanya Israeli kufanya dhambi. 19 Kisha Pulu mfalme wa Ashuru
akaja kinyume cha nchi, na Menahemu akampatia Pulu talanta elfu moja za fedha,
hivyo msaada wa Pulu ungeweza kuwa na yeye kuimarisha utawala wa Israeli katika
nchi yake. 20 Menahemu akatoza hii pesa kutoka Israeli kwa kumtaka kila mtu
tajiri alipe shekeli hamsini za fedha kwake kumpatia mfalme wa Ashura. Hivyo
mfalme wa Ashuru akarudi na hakukaa pale katika ile nchi. 21 Kama kwa mabo
mengine yanayomuhusu Menahemu, na yote aliyoyafanya, je hayajaandikwa kwenye
kitabu cha matukio ya waflme wa Israeli? 22 Hivyo Menahemu akalala pamoja na
babu zake, na Pekahia mtoto wake akawa mfalme katika mahala pake. 23 Katika
mwaka wa hamsini wa Azaria mfalme wa Yuda, Pekahia mwana wa Menahemu
akaanza kutawala juu ya Israeli katika Samaria; alitawala kwa muda wa miaka
miwili. 24 Alifanya yaliyo maovu usoni pa Yahwe. Hakuziacha dhambi za Yeroboamu
mwana wa Nabeti, ambazo kwa hizo alisababisha Israeli kufanya dhambi. 25 Pekahia
alikuwa na afisa aliyekuwa anaitwa Peka mwana wa Remalia, ambaye alifanya
njama dhidi yake. Pamoja na watu hamsini wa Gileadi, Peka akamuua Pekahia
pamoja na Argobu na Arie katika Samaria, katika ngome ya nyumba ya mfalme.
Peka akamuua alipomua Pekahia akawa mfalme katika mahala pake. 26 Kama kwa
mambo mengine yanayomuhusu Pekahia, yote aliyoyafanya, yameandikwa kwenye
kitabu cha matukio ya wafalme wa Israeli. 27 Katika mwaka wa hamsini na mbili
wa Azia mfalme wa Yuda, Peka mwana wa Remalia akaanza kutawala juu ya Israeli
katika Samaria; alitawala miaka Ishirini. 28 Alifanya yaliyo maovu usoni mwa Yahwe.
Hakuziacha dhambi za Yeroboamu mwana wa Nabati, ambaye alisababisha Israeli
kufanya dhambi. 29 Katika siku za Peka mfalme wa Israeli, Tiglath Pileseri mfalme wa
Ashuru akaja na kuichukua Iyoni, Abel Beth Maaka, Yanoa, Kadeshi, Hazori, Gileadi,
na nchi yote ya Naftali. Akawachukua hao watu hadi Ashuru. 30 Hivyo Hoshea
mwana wa Ela akafanya njama dhidi ya Peka mwana wa Remalia. Akaishambulia
na kisha kumuua. Kisha akawa mfalme katika mahali pake, katika mwaka wa
ishirini wa Yothamu mwana wa Uzia. 31 Kama kwa mambo mengine yanayomuhusu
Peka, yote aliyoyafanya, yameandikwa kwenye kitabu cha matukio ya wafalme wa
Israeli. 32 Katika mwaka wa pili wa Peka mwana wa Remalia, mfalme wa Israeli,
Yothamu mwana wa Azaria, mfalme wa Yuda akaanza kutawala. 33 Alikuwa na umri
wa miaka ishirini alipoanza kutawala; alitawala kwa muda wa miaka kumi na sita
katika Yerusalimu. Mama yake alikuwa anaitwa Yerusha; alikuwa binti ya Sadoki.
34 Yotahmu alifanya yaliyo sahihi usoni pa Yahwe. Alifuata mfano wa yote baba
yake Azaria aliyofanya. 35 Ila, mahali pa juu hapakuchukuliwa. Watu walikuwa
wakitio sadaka na kufukiza ubani katika mahali pa juu. Yothamu akajenga lango la
juu la nyumba ya Yahwe. 36 Kama kwa mambo mengine yanayomuhusu Yothamu, na
yote aliyoyafanya, je yameandikwa katika kitabu cha matukio ya wafalme wa Yuda?
37 Katika zamani hizo Yahwe akaanza kumtuma dhidi ya Yuda Rezini mfalme wa
Sahmu, na Peka mwana wa Remalia. 38 Yothamu akalala pamoja na babu zake na
akazikwa pamoja na babu zake katika mji wa Daudi, babu yake. Kisha Ahazi, mtoto

wake, akwa mfalme katika mhali pake.

# 16

[1] Katika mwaka wa kumi na saba wa Peka mwana wa Pemalia, Ahazi mwana
wa Yothamu mfalme wa Yuda, akaanza kutawala. [2] Ahazi alikuwa na umri wa
miaka ishirini alipoanza kutawala, na alitawala kwa muda wa miaka kumi na sita
katika Yerusalemu. Alifanya yasiyo haki usoni mwa Yahwe Mungu wake, kama
Daudi babu yake. [3] Badala yake, akatembea katika njia ya wafalme wa Israeli;
hasa, akamuweka mwanaye kwenye moto kama sadaka ya kuteketeza, kufuatana na
machukizo ya mataifa, ambayo Yahwe aliwafukuza wana wa Israeli. [4] Akatoa sadaka
na kuchoma ubani mahali pa juu, juu ya milima, na chini ya kila mti mbichi. [5] Kisha
Riseni, mfalme wa Shamu na Peka mwana wa Remalia, mfalme wa Israeli, wakaja
mpaka Yerusalemu kuteka. Wakamzunguka Ahazi, lakini hawakuweza kumshinda.
[6] Katika kipindi hicho, Resini mfalme wa Shamu akamponya Elathi kwa Shamu na
kuwapeleka watu wa Yuda nje ya Elathi. Kisha Washami wakaja kwa Elathi ambapo
waliishi hadi leo. [7] Hivyo Ahazi akatuma wajumbe kwenda kwa Tiglath Pileseri
mfalme wa Ashuru, akisema, “Mimi ni mtumishi wako na mwanao. Panda juu na
uniokoe kutoka kwenye mikononi ya mfalme wa Shamu na kutoka kwenye mkono
wa mfalme wa Israeli, ambao wameniteka.” [8] Hivyo Ahazi akachukua fedha na
dhahabu iliyokuwa imepatikana katika nyumba ya Yahwe na mingoni mwa waweka
hazina wa nyumba ya mfalme na kuituma kama zawadi kwa mfalme wa Ashuru.
[9] Kisha mfalme wa Ashuru akamsikiliza, na mfalme wa Ashuru akaenda juu dhidi ya
Damaski, akaishinda na kuwabeba watu wake kama wafungwa hadi Kiri. Akamuua
Resini pia yule mfalme wa Shamu. [10] Mfalme Ahazi akaenda Dameski kuonana na
Tiglath Pileseri mfalme wa Ashuru. akaiona mdhabahu huko Damski. Akampelekea
Uria kuhani mfano wa ile madhabahu na mpangilio wake na mchoro kwa ustadi
wote ulikuwa umehitajika. [11] Hivyo Uria yule kuhani akajenga madhabahu kuwa
kama mipango ambayo Mfalme Ahazi atakaporudi kutoka Damaski. Akaimaliza
kabla mfalme Ahazi hajarudi kutoka Dameski. [12] Kisha mfalme akaja kuto Dameski
akaiona ile madhabahu; mfalme akaikaribia ile madhabahu na kutoa sadaka juu
yake. [13] Akatengeneza sadaka yake ya kuteketezwa na sadaka yake ya nafaka, na
kunyunyiza damu ya washirika wake sadaka juu ya madhabahu. [14] Madhabahu ya
shaba ambayo ilikuwa mbele ya Yahwe-akaileta kutoka mbele ya hekalu, kutoka
kati ya madhabahu yake na hekalu la Yahwe na kuiweka upande wa kaskazini
wa madhabahu yake. [15] Kisha mfalme Ahazi akamwiamuru Uria kuhani, akisema,
“Juu ya madhabahu kubwa teketeza sadaka ya kutekezwa ya asubuhi na sadaka ya
kuteketezwa ya nafaka ya jioni, pamoja na sadaka ya watu wote wa nchi, na matoleo
ya sadaka ya mazao na sadaka zao za kinywaji. Nyunyiza juu ya hiyo damu yote
ya sadaka ya kuteketeza, na damu yote ya kuteketeza. Lakini ile madhabahu ya
shaba itakuwa kwa ajili yangu ili niulize ushauri.” [16] Uria kuhani akafanya kile
ambacho Ahazi aliamuru. [17] Kisha mfalme Ahazi akaondoa jopo na mabeseni vitako
vinavyobebeka; pia akachukua bahari kutoka juu ya ng'ombe wa shaba ambayo
ilikuwa chini ya hiyo na kuiweka juu ya sakafu ya mawe. [18] Aliondoa njia iliyokuwa
kwa ajili ya kuingia kwenye Sabato ambayo walikuwa wamejenga kwenye hekalu,
wote pamoja na mahali pa kuingilia mfalme kwenye hekalu la Yahwe, kwasababu
ya mfalme wa Ashuru. [19] Kama kwa mambo mengine yanayomuhusu Ahazi na yale
aliyoyafanya, je yameandikwa kwenye kitabu cha matukio ya wafalme wa Yuda?
[20] Ahazi alilala pamoja na babu zake na kuzikwa pamoja babu zake katika mji wa
Daudi. Hezekia mtoto wake akawa mfalme katika mahala pake.

# 17

1 Katika mwaka wa kumi na moja wa Ahazi mfalme Yuda, utawala wa Hoshea
mwana wa Elahi ulianza. Alitawala katika Samaria juu ya Israeli kwa muda wa
miaka minane. 2 Alifanya yaliyo maovu usoni pa Yahwe, ila sio kama waflme wa
Israeli ambao ulikuwa kabla yake. 3 Shalmanesa mfalme wa Ashuru akamshambulia,
na Hoshea akawa mtumishi na kumletea kodi. 4 Kisha mfalme wa Ashuru akaona
kwamba Hoshea alikuwa na njama dhidi ya yake, kwa kuwa Hoshea aliwatuma
wajumbe kwa So mfalme wa Misri; pia, hakumpatia kodi mfalme wa Ashuru, kama
alivyofanya mwaka hadi mwaka. 5 Basi mfalme wa Ashuru akamfunga akamtia
kifungoni. Kisha mfalme wa Ashuru akaishambulia nchi yote, akaishambulia
Samaria na kuizunguka kwa miaka mitatu. 6 Katika mwaka wa tisa wa Hoshea,
mfalme wa Ashuru akaichukua Samaria na akawapeleka Israeli hadi Ashuru.
Akawaweka kwenye Hala, kwenye Habori Mto wa Gozani, na katika mji wa Wamedi.
7 Utekwaji huu ulitokea kwa sababu wana wa Israeli walifanya dhambi dhidi ya
Yahwe Mungu wao, ambaye aliwaleta kutoka nchi ya Misri, kutoka chini ya mkono wa
Farao mfalme wa Misri. Watu walikuwa wakiabudu miungu mingine 8 na kutembea
katika matendo ya wamataifa ambao Yahwe aliwafukuza mbele ya watu wa Israeli,
na katika matendo ya wafalme wa Israeli ambayo waliyokuwa wameyafanya.
9 Wana wa Israeli wakafanya kwa siri mambo mabaya dhidi ya Yahwe Mungu wao.
Wakajijengea mahala pa juu katika miji yao yote, kutoka mnara wa walinzi hadi mji
wenye boma. 10 Pia wakasimamisha nguzo za mawe na Ashera juu ya kila mlima
chini ya kila mti mbichi. 11 Huko wakafukiza ubani katika mahali pa juu pote, kama
mataifa walivyokuwa wamefanya, ambao Yahwe aliwafukuza mbele yao. Waisraeli
wakafanya mambo maovu ili kuchochea hasira ya Yahwe, 12 wakaabudu sanamu,
ambazo Yahwe alizokuwa amewaambia, "Msifanye jambo hili." 13 Bado Yahwe
aliwashuhudia Israeli na Yuda kwa kila nabii na kila muonaji, kusema, "Geukeni
kutoka nija zenu mbaya na kuzishika amri zangu na hukumu zangu, na kuwa
makini kufuata ile sheria yote niliyowaamuru baba zenu, na ambayo niliwapelekea
kwa watumishi wangu manabii." 14 Lakini hawakuweza kusikia; badala yake
walikuwa wakaidi kama baba zao ambao hawakumwamini Yahwe Mungu wao.
15 Walizikataa sheria zake na lile agano ambalo alililifanya pamoja na babu zao, na
hilo agano wakakubaliana wapewe. Wakafuata mambo yao yasiyofaa na wakawa
hawafai. Wakawafuata mataifa ya kipagani ambao waliwazunguka, ambao Yahwe
alikuwa amewaamuru wasiige. 16 Wakazipuuza amri zote za Yahwe Mungu wao.
Wakatengeneza sanamu za kusubu za ndama wawili kuziabudu. Wakatengeza nguzo
ya Ashera, na wakaziabudu nyota zote za mbinguni na Baali. 17 Wakawatupia watoto
wao wakike kwa wakiume kwenye moto, wakapiga ramli na uchawi, wakajiuza
wenyewe kufanya yale ambayo yalikuwa maovu usoni pa Yahwe, na kuichochea
hasira yake. 18 Kwa hiyo Yahwe alikuwa na hasira na Israeli na kuwaondoa usoni
mwake. Hakubakia mtu hata mmoja isipokuwa kabila la Yuda peke yake. 19 Hata
watu wa Yuda hawakushika amri za Yahwe Mungu wao, lakini badala yake walifuata
mambo hayo hayo ya kipagani ambayo Israeli walifuata. 20 Hivyo Yahwe akawakataa
vizazi vyote vya Israeli; akawatesa na kuwatia kwenye mkono wa wale wenye
kuwateka nyara, hadi atakapokuwa amewatupa usoni mwake. 21 Akawatoa Israeli
kutoka kwenye mstari wa kifalme wa Daudi, na wakamfanya Yeroboamu mwana wa
Nabeti mfalme. Yeroboamu akawapeleka Israeli mbali kutoka kumfuata Yahwe na
kuwafanya wafanye dhambi kubwa. 22 Wana wa Israeli wakafuata dhambi zote za
Yeroboamu na hawakujiepusha nazo, 23 basi Yahwe akawaondoa Israeli kutoka usoni
pake, kama alivyokuwa amesema kupitia watumishi wake wote manabii kwamba
angeweza kufanya. Hivyo Israeli walichukuliwa kutoka nchi yao kwenda Ashuru, na

iko hivyo hata leo. 24 Mfalme wa Ashuru akawaleta watu kutoka Babeli na kutoka
Kutha, na kutoka Ava, na kutoka Hamathi na Sefarvaimu, na kuwaweka katika mji
wa Samaria na kuishi katika huo mji wake. 25 Ikatokea wakati walipoanza kuishi
huko hawakumcha Yahwe. Hivyo Yahwe akatuma simba miongoni mwao ambao
waliwaua baadhi yao. 26 Basi wakaongea na mfalme wa Ashuru, wakisema, “Wale
mataifa uliowaamisha na kuwaweka kwenye miji ya Samaria hawayajui mambo
wanayotakiwa kuyafanya kutokana na mungu wa nchi. Hivyo alikuwa amewatuma
simba kwenda kwao, na, tazama, wale simba walikuwa wakiwauua watu huko
kwa sababu hawakufahamu yale mambo waliyokuwa wanatakiwa kuyafanya kwa
mungu wa nchi.” 27 Kisha mfalme wa Ashuru akatoa amri, akisema, “Mchukueni
mmoja wa makuhani hapo ambaye mmemleta kutoka huko, na mumwache aende
na kuishi huko, na mumwache awafundishe mambo yanayotakiwa kwa mungu wa
nchi.” 28 Hivyo mmoja wa makuhani ambaye walimchukua kutoka Samaria akaja
na kuishi katika Betheli; akawafundisha jinsi wavyotakiwa mcha Yahwe. 29 Watu wa
kila kabila wakajifanyia miungu yao wenyewe, na kuiweka mahala pa juu ambapo
Wasamaria walifanya kila kabila katika mji ambako walipoishi. 30 Watu wa Babeli
wakatengeneza Sakoth Benithi; watu wa Sakoth wakatengeneza Nergali; watu wa
Hamathi wakatengeza Ashima; 31 Waavi wakatengeneza Nibhazi na Tartaki. Nao
Wasefarvi wakwachoma watoto wao kwenye moto kwa Adrameleki na Anameleki,
wale miungu wa Sefarvaimu. 32 Pia wakamcha Yahwe, na kuwateua kutoka miongoni
mwao makuhani wa mahali pa juu, ambao waliteketeza kwa ajili yao kwenye hekalun
mahali pa juu. 33 Wakamcha Yahwe na pia kuabudu miungu yao wenyewe, sawa
sawa na tamaduni za mataifa kutoka miongoni mwao waliokuwa wamewachukua.
34 Hadi siku hii ya leo wameshikilia tamaduni zao za zamani. Wala hawamwogopi
Yahwe, wala hawazifuati sheria zake, torati, au amri ambazo Yahwe aliwapa watu
wa Yakobo ambaye alemwita jina Israeli 35 pamoja na ambao Yahwe alifanya agano
nao na kuwaamuru, “Msiiche miungu mingine, wala kuisujudia, wala kuiabudu,
wala kuitolea sadaka. 36 Lakini Yahwe, ambaye aliwatoa kutoka nchi ya Misri kwa
nguvu kubwa na mkono ulionyooshwa, yeye ndiye mnayetakiwa kumwabudu, yeye
ndiye manayetakiwa kumsujudia, na yeye ndiye mnayetakiwa kumtolea sadaka.
37 Na sheria na hukumu, na torati na amri ambazo alizoziandika kwa ajili yenu,
mtazishika milele. Hivyo msiiche miungu mingine, 38 na agano ambalo nimelifanya
pamoja nanyi, hamtalisahau; wala kuicha miungu mingine. 39 Lakini Yahwe Mungu
wenu, ndiye ambaye mtakayemcha. Atawalinda mbali na nguvu ya maadui zenu,”
40 Hawatasikia, kwasababu waliendelea kufanya yale waliyokuwa wameyafanya
nyuma. 41 Hivyo haya mataifa wakamcha Yahwe na pia wakaabudu sanamu zao
za kuchonga, na watoto wao wakafanya hivyo hivyo na watoto wa watoto wao.
Wakaendelea kufanya yale ambayo babu zao waliyoyafanya, hata leo.

# 18

1 Ikawa katika mwaka wa tatu wa Hoshea mwana wa Ela, mfalme wa Israeli,
Hezekia mwana wa Ahazi, mfalme wa Yuda akaanza kutawala. 2 Alikuwa na umri
wa miaka ishirini na tano alipoanza kutawala; alitawala miaka ishirini na tisa katika
Yerusalemu. Jina la mama yake alikuwa anaitwa Abija; alikuwa binti wa Zekaria.
3 Alifanya yaliyo mema usoni pa Yahwe, kufuata mfano wa yote ambayo Daudi, babu
yake, aliyoyafanya. 4 Alipaondoa mahali pa juu, akaiharibu nguzo ya jiwe, akaikata
hiyo nguzo ya Ashera. Akavunja vipande vipande ile nyoka ambayo Musa aliyokuwa
ameifanya, kwa sababu siku zile wana wa Israeli walikuwa wakichoma ubani katika
hiyo; ilikuwa inaitwa “Nehushtani.” 5 Hezekia alimwamini Yahwe, Mungu wa Israeli,
hivyo basi baada ya yeye hapakuwa kama yeye miongoni mwa wafalme wote wa

Yuda, wala miongoni mwa wafalme ambao walikuwa kabla yake. [6] Aliambatana na
Yahwe. Hakuacha kumfuata lakini alizifuata amri zake, ambazo Yahwe alimwamuru
Musa. [7] Hivyo Yahwe alikuwa na Hezekia, kila alipokwenda alifanikiwa. Akaasi dhidi
ya mfalme wa Ashuru na hakumtumikia. [8] Akawashambulia Wafilisti hadi Gaza
na mipaka inayoizunguka, kutoka mnara wa walinzi hadi hadi mji wenye ngome.
[9] Katika mwaka wa nne wa Mfalme Hezekia, ambao ulikuwa mwaka wa saba wa
Hoshea mwana wa Ela mfalme wa Israeli, Shalmanesa mfalme wa Ashuru akapanda
hadi Samaria na kuizunguka. [10] Mwishoni mwa miaka mitatu wakaichukua, katika
mwaka wa sita wa Hezekia, ambao ulikuwa mwaka wa tisa wa Hoshea mfalme wa
Israeli; hivi ndivyo Samaria ilivyotekwa. [11] Basi mfalme wa Ashuru akawachukua
Israeli kwenda Ashuru na kuwaweka kwenye Hala, na katika mto Habori katika
Gozani, na katika mji wa Wamedi. [12] Alifanya hivi kwasababu hakutii sauti ya
Yahwe Mungu wao, lakini walikiuka makubaliano ya agano lake, yote yale ambayo
Musa yule mtumishi wa Yahwe aliwaamuru. Walikataa kuyasikiliza au kuyafanya.
[13] Kisha katika mwaka wa kumi na nne wa mfalme Hezekia, Senakerebu mfalme
wa Ashuru akaishambulia miji yote yenye boma na kuwateka mateka. [14] Basi
Hezekia mfalme wa Yuda akatuma neno kwenda kwa mfalalme wa Yuda akatuma
neno kwa mfalme wa Ashuru, ambaye alikuwa Lachishi, akisema, “Nimekuudhi.
Nichukue. Popote utakaponiweka nitavumulia”. Mfalme wa Ashuru akamtaka
Hezekia mfalme wa Yuda kulipa talanta mia tatu za fedha na talanta thelathini za
dhahabu. [15] Hivyo Hezekia akampatia fedha zote ambazo zilikuwa zimepatikana
kwenye nyumba ya Yahwe na kawenye hazina nyumba ya mfalme. [16] Kisha Hezekia
akaikata ile dhahabu kutoka kwenye milango ya hekalu la Yahwe na kutoka juu
ya nguzo; akampatia dhahabu mfalme wa Ashuru. [17] Lakini mfalme wa Ashuru
akalihamasisha jeshi lake kubwa, akawatuma Tartani na Rabsarisi na amiri jeshi
mkuu kutoka Lakishi kwenda kwa Hezekia huko Yerusalemu. Wakasafiri hadi
kwenye mabarabara na kufika nje ya Yerusalemu. Wakakaribia karibu na mfereji wa
birika la juu, kwenye barabara kuu ya shamba la dobi, na kusimama hapo. [18] Wakati
walipokuwa wamemwita Mfalme Hezekia, Eliakimu mwana wa Hilkia, ambaye
alikuwa kiongozi wa nyumba ya mfalme na Shebna mwandishi, na Joa mwana
wa Asafu, anayeandika kumbukumbu, wakatoka nje kwenda kuwalaki [19] Basi yule
amiri jeshi mkuu akawaambia wamwambie Hezekia kile alichosema mfalme mkuu,
mfalme wa Ashuru, amesema: “Nini chanzo cha ujasiri wako? [20] Unaongea maneno
yasiyo na maana, kusema lipo neno na nguvu ya vita. Sasa unamtumainia nani? Nani
anakupa ujasiri wa kuasi dhidi yangu? [21] Tazama, unatumainia kutembelea fimbo
ya mwanzi huu uliopondeka wa Misri, lakini kama mtu akiutegemea, utamchapa
kwenye mkono wake na kuutoboa. Hicho ndicho Farao mfalme wa Misri kwa ymtu
yeyote ambaye anayemtumainia. [22] Lakini kama ukiniambia, 'Tunamwamini Yahwe
Mungu watu; je si yeye ambaye mahali pa juu na madhabahu Hezekia amezichukua,
na kumwambia Yuda na kwa Yerusalemu, 'Lazima uabudu mbele ya hii madhabahu
katika Yerusalemu'? [23] Basi kwa hiyo, nataka kukufanyia ahadi nzuri kutoka kwa
bwana wangu mfalme wa Ashuru. Nitakupatia farasi elfu mbili, kama unaweza
kuwatafuta kuwaendesha kwa ajili yao. [24] Wanawezaje kumpinga hata nahodha
mmoja wa watumishi walio wadogo? Mmeweka tumaini lenu katika Misri kwa
magari ya farasi na waendesha farasi! [25] Je nimesafiri kwenda huko juu bila Yahwe
kupapigania hapa mahali na kupaharibu? Yahwe ameniambia, 'Ishambulie hii nchi
na uiharibu.”' [26] Kisha Elikana mwana wa Hilkia, na Shebna, na Joa wakamwambia
amiri jeshi mkuu, “Tafadhali ongea na watumishi wako katika lugha ya Kiaramu,
kwa kuwa tunaielewa. Usiongee nasi katika lugha ya Yuda katika masikio ya watu
ambao wako ukutani.” [27] Lakini yule amiri jeshi mkuu akawaambia, “Je bwana

wangu amenituma kwa bwana wako na kuwachukua kuongea haya maneno? Je
hajanituma kwa hawa watu ambao wameketi kwenye ukuta, ambao watakula kinyesi
chao na kunywa mkojo wao wenyewe?” 28 Kisha yule amiri jeshi mkuu akasimama na
akapiga kelele kubwa kwa lugha ya Kiyahudi, akisema, “Sikilizeni neno la mfalme
mkuu, mfale wa Ashuru. 29 Mfalme asema, 'Msimwache Hezekia akawadanganya,
kwa kuwa hataweza kuwaokoa kwenye nguvu yangu. 30 Msimwache Hezekia
akawatumainisha katika Yahwe, akisema, “Yahwe atatuokoa hakika, na huu mji
hautawekwa kwenye mkono wa mfalme wa Ashuru.'” 31 Msikilize Hezekia, kwa kuwa
hivi ndivyo mfalme wa Ashuru asemavyo: 'Fanyeni amani pamoja nami na njooni
kwangu. Kisha kila mmoja wenu atakula kutoka kwenye mzabibu wake mwenyewe
na kutoka kwenye mtini wake mwenyewe, na kunywa kutoka kwenye maji kwenye
maji ya birika lake mwenyewe. 32 Mtafanya hivyo hadi nitakapokuja na kuwachukua
kwenda kwenye nchi kama nchi yenu, nchi ya nafaka na divai, nchi ya mkate
na mashamba ya mizabibu, nchi ya miti ya mizaituni na asali, ili muweze kuishi
na sio kufa.' Msimsikilize Hezekia wakati atakapojaribu kuwashawishi, akisema,
'Yahwe atatuokoa.' 33 Je miungu yeyote ya watu inayewaokoa kutoka kwenye nchi
ya mfalme wa Ashuru? 34 Iko wapi miungu ya Hamathi na Arpadi? iko wapi
miungu ya Sefarvaimu, Hena, na Iva? Je imeiokoa Samaria kutoka mkono wangu?
35 Miongoni mwa miungu yote ya nchi, je kuna mungu ambaye ameiokoa nchi
yake kutoka kwenye nguvu yangu? Inawezekanaje Yahwe akaiokoa Yerusalemu
kutoka kwenye uwezo wangu?” 36 Lakini watu wakabaki kimya na hawakujibu,
kwa kuwa mfalme alikuwa ameamuru, “Msimjibu.” 37 Kisha Eliakimu mwana wa
Hilkia, ambaye alikuwa juu ya nyumba ya mfalme; Shebna yule mwandishi; na Joa
mwana wa Asafu, mtunza kumbukumbu, akaja kwa Hezekia pamoja na nguo zao
zilizoraruliwa, na kumpatia taarifa ya maneno ya yule amiri mkuu.

# 19

1 Ikawa kuhusu kwamba wakati Mfalme Hezekia aliposikia taazrifa zao, akararua
mavazi yake, akavaa nguo za magunia, na kwenda kwenye nyumba ya Yahwe.
2 Akamtuma Elkana, ambaye alikua msimamizi wa nyumba ya mfalme, na Shebna
yule mwandishi, na wazee wa makuhani, wote walikuwa wamefunikwa na nguo
za magunia, kwenda kwa Isaya mwana wa Amozi, yule nabii. 3 Wakamwambia,
“Hezekia wakisema, 'siku hii ni siku ya mateso, shutuma, na fedheha, kwa kuwa
wakati umewadia watoto kuzaliwa, lakini hakuna nguvu ili wazaliwe. 4 Inaweza
kuwa Yahwe Mungu wako atasikia maneno yote ya amiri jeshi mkuu, ambaye mfalme
wa Ashuru bwana wake amemtuma kumkaidi Mungu aliye hai, naye atayakemea
yale maneno ambayo Yahwe Mungu wako aliyasikia. Sasa inua maombi yako juu
kwa ajili ya mabaki yaliyo bakia hapo.”' 5 Hivyo watumishi wa mfalme Hezekia
wakaja kwa Isaya, 6 na Isaya akawaambia, “Mwambieni bwana wenu: 'Yahwe asema
hivi, “Usiyaogope maneno ambayo uliyoyasikia, pamoja na kwamba watumishi wa
mfalme wa Ashuru wamenitukana. 7 Tazama, nitaweka roho ndani yake, na yamkini
atasikia taarifa na kurudi kwenye nchi yake mwenyewe. Nitamfanya aanguke
kwa upanga katika nchi yake mwenyewe."”' 8 Kisha amiri jeshi mkuu akarudi na
kumkuta mfalme wa Ashuru akipigana dhidi ya Libna, kwa kuwa alisikia kwamba
mfalme alikuwa ameenda kutoka Lakishi. 9 Kisha Senakeribu akasikia kwamba
Tirhaka mfalme wa Kushi na Misri alihamasisha kupigana dhidi yake, hivyo akatuma
wajumbe tena kwa Hezekia pamoja na ujumbe: 10 “Mwambieni Hezekia mfalme
wa Yuda, 'Asikudanganye Mungu wako unayemwamini, kusema, “Yerusalemu
haitawekwa kwenye mikono ya mikono ya mfalme wa Ashuru.” 11 Tazama, umesikia
kwamba wafalme wa Ashuru wamemaliza nchi zote kwa kuziharibu kabisa. Kwa

hiyo je utaokoka? [12] Je wale miungu wa mataifa wamewaokoa, mataifa ambao baba
zangu waliyaharibu: Gozani, Harani, Resefu, na watu wa Edeni katika Telasari? [13] Je
yuko wapi mfalme wa Hamathi, mfalme Arpadi, mfalme wa miji ya Sefarvaimu,
wa Hena, na Iva?"' [14] Hezekia akapokea hii barua kutoka wale wajumbe na
kuisoma. Kisha akapanda hata kwenye nyumba ya Yahwe na kuukunjua mbele
yake. [15] Kisha Hezekia akaomba mbele ya Yahwe na kusema, "Yahwe wa majeshi,
Mungu wa Israeli, uketiye juu ya makerubi, wewe ni Mungu wa pekee juu ya
tawala zote za dunia. Uliyeziumba mbingu na nchi. [16] Tega sikio lako, Yahwe, na
usikie. Fungua macho yako, Yahwe, na tazama, na sikia maneno ya Senakeribu,
ambayo ameyatuma kumdhihaki Mungu aliye hai. [17] Ni kweli, Yahwe, wafalme
wa Ashuru ameyaharibu mataifa na nchi zao. [18] Wameiweka miungu yao kwenye
moto, kwa kuwa hawakuwa miungu lakini ilikuwa kazi ya mikono ya watu, ilikuwa
miti na mawe. Hivyo Waashuru wamewaharibu. [19] Basi sasa, Yahwe Mungu wetu,
tuokoe, nakusihi, kutoka kwenye nguvu zake, ili kwamba mamlaka zote za dunia
zipate kujua yakwamba wewe, Yahwe, ndiye Mungu wa pekee." [20] Kisha Isaya
mwana wa Amozi akatuma ujumbe kwa Hezekia, akisema, "Yahwe, Mungu wa Israeli
asema, 'Kwasababu umeomba kwangu kuhusiana na Senakeribu mfalme wa Ashuru,
nimekusikia. [21] Hili ndilo neno ambalo Yahwe ameliongea kuhusu yeye: "Bikira
binti Sayuni amekudharau na kukucheka kwa dharau. Binti wa Yerusalemu akatikisa
kichwa juu yako. [22] Je ni nani uliyemchokoza na kumtukana? Dhidi ya nani umeinua
sauti yako na kuinua macho yako katika majivuno? Juu ya Mtakatifu wa Israeli!
[23] Kupitia wajumbe wako wamemdharau Bwana, na kusema, 'Pamoja na wingi wa
magari yangu ya farasi nimeenda juu ya vilele ya milima, hata juu ya kilele cha
Lebanoni. Nitaikata mierezi mirefu na kuchagua miti ya mivinje huko. Nitaingia
sehemu za makazi yake yaliyo mbali, msitu wake uzaao sana. [24] Nimechimba visima
na kunywa maji mageni. Nimekausha mito yote ya Misri chini ya soli ya miguu
yangu.' [25] Je hukusikia jinsi nilivyoagiza tangu zamani, na kuyafanya tangu siku
za zamani? Sasa ninalileta kupita. Uko hapa kupunguza miji isiyoingilika kwenye
rundo la maangamizi. [26] Makazi yao, ya nguvu kidogo, imevunjwa vunjwa na aibu.
Wamekuwa mimea katika shamba, majani ya kijani, majani juu kwenye dari au
kwenye shamba, lililochomwa kabla halijakua. [27] Lakini najua kuketi kwako chini, na
kutoka kwako, kuingia kwako dhidi yangu. [28] Kwasababu kiburi chako kimeyafikia
masikio yangu, Nitaweka kulabu yangu kwenye pua yako, na hatamu yangu kwenye
mdomo wako; nitakurudisha nyuma kwa njia ile ile uliyoijia." [29] Hii ndiyo itakuwa
ishara kwako: Mwaka huu mtakula vitu viotavyo porini, na katika mwaka wa pili
vile vikuavyo katika huo. Lakini katika mwaka wa tatu ni lazima mpande na kuvuna,
kupanda mashamba ya mizabibu na kula matunda yake. [30] Mabaki ya nyumba ya
Yuda ambayo yataokoka yatachukua tena mizizi na kuzaa matunda. [31] Kwa kuwa
mabaki yatatoka Yerusalemu, kutoka Mlima Sayuni wenye kuokoka utakuja. Wivu
wa Yahwe wa majeshi utafanya hivyo. [32] Kwa hiyo Yahwe asema hivi kuhusu mfalme
wa Ashuru: "Hatakuja kwenye huu mji wala kupiga mshale hapa. Wala hatakuja
mbele yake na ngao au kujenga boma dhidi yake. [33] Njia ile ile aliyoijia ndiyo njia
atakayoondokea; hatoingia mji huu - hivi ndivyo asemavyo Yahwe." [34] Kwa maana
nitaulinda huu mji na kuuokoa, kwa ajili yangu mwenyewe na kwa ajili ya Daudi
mtumishi wangu."' [35] Ikawa kuhusu usiku huo ambao malaika wa Yahwe alitoka
na kuvamia kambi ya Waashuru, akawaua maaskari185, 000. Kisha watu wakaamka
asubuhi na mapema, miili ya watu waliokuwa wamekufa ilikuwa imelala kila mahali.
[36] Hivyo Senakeribu mfalme wa Ashuru akaondoka Israeli na kwenda nyumbani na
kuishi katika Ninawi. [37] Baadaye, alipokuwa akiabudu kwenye nyumba ya Nisroki
mungu wake, watoto wake Adramaleki na Shareza wakamuua kwa upanga. Kisha

wakakimbilia kwenye nchi ya Ararati. Kisha Esarhodani mwanaye akawa mfalme
katika mahali pake.

## 20

1 Katika siku hizo Hezekia aliugua akawa kwenye hatari ya kufa. Hivyo Isaya
mwana wa Amozi, akaja, na kumwambia, “Yahwe asema, 'Weka nyumba yako
kwenye mpangilio; kwa kuwa utakufa, na hutapona.'” 2 Kisha Ahazi akageuza uso
wake kwenye ukuta na kumuomba Yahwe, akisema, 3 “Tafadhali, Yahwe, ukumbuke
jinsi nilivyo mwaminifu kutembea mbele yako kwa moyo wangu wote, na jinsi
nilivyofanya yaliyo mazuri usoni kwako.” Kisha Hezekia akalia kwa sauti. 4 Kabla
ya Isaya hajatoka nje kwenye mji wa kati, neno la Yahwe likamjia, kusema, 5 '“Rudi,
na umwambie Hezekia, kiongozi wa watu wangu, 'Hivi ndivyo Yahwe, Mungu wa
Daudi babu yako, asemavyo: “Nimesikia maombi yako, na nimeyaona machozi
yako. Nitakuponya katika siku ya tatu, na utapanda juu kwenye nyumba ya Yahwe.
6 Nitakuongeza miaka kumi na tano ya maisha yako, na nitakulinda na huu mji kwa
ajili yangu na kwa ajili ya mtumishi wangu."”' 7 Hivyo Isaya akasema, “Chukueni
mkate wa tini.” Walifanya hivyo na kuweka kwenye jipu lake, na akapona. 8 Hezekia
akamwambia Isaya, “Je kutakuwa na alama gani ambayo Yahwe ataniponya, na
kwamba nitapanda juu hadi kwenye hekalu la Yahwe katika siku ya tatu?” 9 Isaya
akajibu, “Hii ndiyo itakuwa ishara kwako kutoka kwa Yahwe, kwamba Yahwe
atafanya kitu amacho alichokisema. Je kivuli kitaenda mbele hatua saba, au kurudi
nyuma hatua saba?” 10 Hezekia akajibu, “Ni kitu chepesi kwa kivuli kwenda
mbele hatua kumi. Hapana, hicho kivuli kirudi nyuma hatua kumi.” 11 Hivyo
Isaya nabii akamlilia Yahwe, na akaleta kivuli hatua kumi nyuma, kutoka pale
ambapo zilikuwa zimevuka kwenye ngazi za Ahazi. 12 Katika kipindi hicho Merodak
Baladani mfalme wa Babeli alituma barua na zawadi kwa Hezekia, kwa kuwa alisikia
kwamba Hezekia alikuwa anaumwa. 13 Hezekia akasikiliza hizo barua, na kisha
kuwaonyesha wajumbe sehemu zote na sehemu zake za thamani, fedha, dhahabu,
manukato na marhamu na nyumba yenye ghala la silaha zake, na yote yaliyokutwa
kwenye ghala za nyumba zake. Hapakuwa na kitu kwenye nyumba, wala kwenye
ufalme wake wote, ambao Hezekia hakuwaonyesha. 14 Kisha Isaya akaja kwa
Hezekia na kumuuliza, “Hawa watu walikuwa wanakwambiaje? Wanatokea wapi?”
Hezekia aksema, “Wamekuja kutoka nchi ya mbali ya Babeli. 15 Isaya akauliza,
“Wameona nini kwenye nyumba yako?” Hezekia akajibu, “Wameona kila kitu
kwenye nyumba yangu. Hakuna kitu miongoni mwa vitu vyangu vya thamani
ambavyo sijawaonyesha.” 16 Basi Isaya akamwambia Hezekia, “Sikiliza neno la
Yahwe: 17 'Tazama siku zinakuja wakati kila kitu kwenye kwenye nyumba yako ya
kifalme, vitu ambavyo babu zako walivitunza huko hadi leo, vitabebwa kwenda
Babeli. Hakuna kitakachobakia, Yahwe asema. 18 Watoto waliozaliwa na wewe,
ambao umewazaa wewe mwenyewe-watawachukua mbali, na watakuwa matowashi
kwenye nyumba ya kifalme ya mfalme wa Babeli.'” 19 Hezekia akamwambia Isaya,
“neno la Yahwe ulililoliongea ni jema.” Kwa kuwa alifikiri, Je sivyo ikiwapo amani na
kweli katika siku zangu?” 20 Kama kwa mambo mengine yanamuhusu Hezekia, na
ushujaa wake wote, na jinsi alivyotengeza bwawa la maji na mfereji, na kuleta maji
kwenye mji-hayakuandikwa kwenye kitabu cha ya matukio ya wafalme wa Yuda?
21 Hezekia akalala na babu zake, na Manase mwanae akawa mfalme katika sehemu
yake.

## 21

1 Manase alikuwa na umri wa miaka kumi na mbili wakati alipoanza kutawala;

alitawala miaka hamsini na tano katika Yerusalemu. Mama yake alikuwa anaitwa
Hefziba. 2 Alifanya maovu usoni kwa Yahwe, kama machukizo ya mataifa ambayo
Yahwe aliyafukuza nje mbele ya wana wa Israeli. 3 Kwa kupajenga tena mahala
pa juu ambapo Hezekia baba yake alipaharibu, na akajenga madhabahu kwa ajili
ya Baali, akafanya Ashera, kama Ahabu mfalme wa Israeli alivyofanya, akasujudu
kwa nyota zote za mbinguni na kuwaabudu wao. 4 Manase akajenga madhabahu za
kipagani kwenye nyumba ya Yahwe, ingawaje Yahwe aliamuru, "Jina langu litakuwa
Yerusalemu daima." 5 Akajenga madhabahu kwa ajili ya nyota zote za mbinguni
katika behewa mbili za nyumba ya Yahwe. 6 Akamuweka mtoto wake wa kiume
kwenye moto; akatazama bao ushirikina na kujishuhulisha pamoja wale ambao
wenye pepo wa utambuzi na wale wachawi. Akafanya maovu mengi usoni kwa
Yahwe na kuchochea hasira kwa Mungu. 7 Sanamu ya kuchongwa ya Ashera ambayo
aliitnegeneza, akaiweka kwenye nyumba ya Yahwe. Nyumba hii ndiyo ambayo
Yahwe alimwambia Daudi na Sulemani mwanawe; alisema: "Ni nyumba hii na
katika Yerusalemu, ambayo nimeichagua kutoka makabila yote ya Isaraeli, ambako
nitaliweka jina langu milele. 8 Sintofanya miguu ya Israeli kushindwa tena nje ya nchi
ambayo niliwapa babu zao, kama tu watakuwa makini kutii yale yote niliyowaamuru,
na kufuata sheria zote ambazo mtumishi wangu Musa aliwaamuru." 9 Lakini watu
hawakusikia, na Manase akawaongoza kufanya maovu zaidi kuliko yale ya mataifa
ambayo Yahwe aliyaharibu mbele ya watu wa Israeli. 10 Basi Yahwe akaongea na
watumishi wake manabii, akisema, 11 Kwasababu Manase mfalme wa Yuda amefanya
haya machukizo, na kutenda maovu zaidi kuliko yote waliyoyatenda Waamori ambao
walikuwa mbele yake walikubali, na pia aliwafanya Yuda kuasi kwa sanamu zake,
12 kwa hiyo Yahwe, Mungu wa Israeli, akasema hivi: Tazama, nakaribia kuleta uovu
juu ya Yerusalemu na Yuda ambayo kila mtu asikiapo kuhusu hilo, masikio yake
yote yatang'aa. 13 Nitanyoosha juu ya Yerusalemu kipimo kilichotumika dhidi ya
Samaria, na kuangusha msatari utakaotumika dhidi ya nyumba ya Ahabu; Nitaifuta
Yerusalemu safi, kama kufuta sahani, kuifuta na kuifunika juu chini. 14 Nitawatupa
masalia ya urithi wangu na kuwaweka mikononi mwa maadui zao. Watakuwa
nyara na mateka kwa maadui zao wote, 15 kwa sababu wamefanya yaliyo maovu
usoni kwangu, na kunichochea hasira, tangu siku babu zao walipotoka Misri, hadi
leo." 16 Aidha, Manase akazimwaga damu nyingi za wasio na hatia, hadi alipoijaza
Yerusalemu kutoka upande huu kwenda mwingine kwa kifo. Hii ilikuwa ni kuongeza
kwenye dhambi ambayo aliifanya Yuda kuasi, wakati walipofanya uovu mbele za
Yahwe. 17 Kama kwa mambo mengine yamhusuyo Manase, yote aliyoyafanya, na
dhambi ambayo aliyoifanya, je haya hayajaandikwa kwenye kitabu cha matukio
cha wafalme wa Yuda? 18 Manase akalala pamoja na babu zake na alizikwa
kwenye bustani ya nyumba yake, katika bustani ya Uza. Amoni mwanawe akawa
mfalme katika sehemu yake. 19 Amoni alikuwa na miaka kumi na mbili alipoanza
kutawala; alitawala miaka miwili katika Yerusalemu. Mama yake alikuwa anaitwa
Meshlemethi; alikuwa binti wa Haruzi wa Yotba. 20 Alifanya yaliyo maovu usoni mwa
Yahwe, kama manase baba yake alivyofanya. 21 Amoni alifuata njia zote ambazo
baba yake alizotembelea na kuabudu sanamu ambazo baba yake aliziabudu, na
kuzisujudia. 22 Akajitenga na Yahwe, Mungu wa baba zake, na hakutembea katika
njia ya Yahwe. 23 Watumishi wa Amoni wakafanya njama dhidi yake na kumuua
mfalme kwenye nyumba yake mwenyewe. 24 Lakini watu wa nchi wakawaua watu
wote waliofanya njama dhidi ya mfalme Amoni, na wakamfanya Yosia mtoto wake
kuwa mfalme katika sehemu yake. 25 Kama ilivyo kwa mambo mengine yamhusuyo
Amoni yale aliyoyafanya, je hayajaandikwa kwenye kitabu cha matukio ya wafalme
wa Yuda? 26 Watu wakamzika kwenye kaburi lake katika bustani ya Uza, na Yosia

mwanawe akawa mfalme katika sehemu yake.

# 22

1 Yosia alikuwa na umri wa miaka minane wakati alipoanza kutawala; alitawala
kwa mda wa miaka thelathini na moja katika Yerusalemu. Mama yake alikuwa
anaitwa Yedida (Alikuwa binti wa Adaye wa Bozkathi). 2 Alifanya yale yaliyo mema
usoni mwa Yahwe. Alitembea kwenye njia zote za Daudi babu yake, na hakugeuka
wala upande wa kulia au kushoto. 3 Ikawa kwamba katika mwaka wa kumi na
nane mfalme Yosia, akamtuma Shafani mwana wa Azalia mwana wa Meshulamu,
mwandishi, kwenye nyumba ya Yahwe, akisema, 4 "Panda juu kwa Hilkia yule kuhani
mkuu na mwambie ahesabu pesa ambazo zilizokuwa zimeletwa kwenye nyumba ya
Yahwe, ambazo walinzi wa hekalu wamezikusanya kutoka kwa watu. 5 Zigawanywe
kwenye mikono ya wafanyakazi ambao ni wasimamizi wa nyumba ya Yahwe, na
waache wawapatie wafanya kazi ambao wako kwenye nyumba ya Yahwe, ili waweze
kutengeneza pale palipoharibika. 6 Wapewe pesa maseremala, wajenzi, na waashi, na
pia kununua mbao na kukata jiwe kukarabati nyumba ya Yahwe." 7 Lakini zile pesa
hazikutakiwa kuhesabiwa wakati walipokuwa wanapewa, kwa sababu waliimudu
ile kazi kwa uaminifu. 8 Hilkia kuhani mkuu akamwambia Shafani yule mwandishi,
"Nimekipata kitabu cha sheria katika nyumba ya Yahwe." Basi Hilkia akampatia
kile kitabu Shafani, na kukisoma. 9 Shafani akaenda na kuchukua kile kitabu
kwa mfalme, na pia kumjulisha, akisema, "Watumishi wako wamezitumia zile pesa
ambazo zilizokuwa zimepatikana kwenye hekalu na zimegawiwa kwenye mikono ya
wafanya kazi ambao husimamia kuangalia nyumba ya Yahwe." 10 Kisha Shafani yule
mwandishi akamwambia mfalme, "Hilkia yule kuhani amenipatia kitabu." Kisha
Shafani akakisoma mbele ya mfalme. 11 Ikawa kwamba wakati mfalme aliposikia
maneno ya sheria, alichana nguo zake. 12 Kisha mfalme akamwamuru Hilkia yule
kuhani, Ahikamu mwana wa Shafani, Akbori mwana wa Mikaya, Shafani mwandishi,
na Asaya, mtumishi wake mwenyewe, akisema, 13 Nenda na ukaongee pamoja na
Yahwe kwa ajili yangu, na kwa ajili ya watu na kwa Yuda yote, kwa sababu ya
maneno ya hiki kitabu ambacho kilichopatikana. Kwa hasira kubwa ya Yahwe
ambayo ametukasirikia dhidi yetu kwa sababu babu zetu hawakusikiliza maneno
ya hiki kitabu hivyo kama kutii yote ambayo yalikuwa yameandikwa kuhusiana
na sisi. 14 Basi Hilkia yule kuhani, Ahikamu, Akbori, Shafani, na Asaya wakaenda
kwa Hulda nabii wa kike, mke wa Shalumu mwana wa Tikva mwana wa Harhasi,
mtunza kabati la nguo (aliishi katika Yerusalemu katika mtaa wa pili), na wakaongea
pamoja naye. 15 Akawaambia, "Hivi ndivyo Yahwe, Mungu wa Israeli, asemavyo:
'Mwambie huyu mtu aliyekutuma kwangu, 16 "Hivi ndivyo Yahwe asemavyo:
'Tazama, nitaleta janga kwenye hii sehemu na juu ya wakaao hapa, kulingana na
kila kitu kilichoandikwa kwenye kitabu ambacho mfalme wa Yuda alichokisoma.
17 Kwa sababu wamenitelekeza na kufukiza ubani kwa miungu mingine, hivyo basi
wanaweza kunichochea hasira pamoja na matendo yote waliyoyafanya-kwa hiyo
hasira yangu ilikuwa inawaka dhidi ya hii sehemu, na haitazimika."' 18 Lakini kwa
mfalme wa Yuda, aliye watuma kuuliza mapenzi ya Yahwe, hivi ndivyo mtakavyo
mwambia: "Yahwe, Mungu wa Israeli asema hivi: Kuhusu yale maneno uliyoyasikia,
19 kwa sababu moyo wako ulikuwa mlaini, na kwa sababu umejinyenyekesha
mwenyewe mbele za Yahwe, wakati uliposikia nilichokisema dhidi ya hii sehemu na
wenyeji wake, kwamba wanaweza kuwa wakiwa na laana, na kwasaabu ulizozirarua
nguo zako na kulia mbele yangu, Nami pia nimekusikia-hivi ndivyo Yahwe asemavyo.
20 Tazama, nitakukusanya na babu zako, nawe utawekwa kaburini kwako kwa amani.

Macho yako hayataona maafa yote ambayo nitayaleta kwenye hii sehemu. “"” Hivyo watu wakachukua ujumbe huu kuurudisha kwa mfalme.

# 23

1 Hivyo mfalme akawatuma wajumbe waliokuwa wamemzunguka wazee wote wa
Yuda na wa Yerusalemu. 2 Kisha mfalme akapanda hadi kwenye nyumba ya Yahwe,
na watu wote wa Yuda na wenyeji wote wa Yerusalemu pamoja naye, na makuhani,
manabii, na watu wote, kuanzia mdogo hadi mkubwa. Kisha akasoma katika
masikioni kwao maneno yote ya kitabu cha agano ambalo lililokuwa limepatikana
kwenye nyumba ya Yahwe. 3 Mfalme akasimama karibu na nguzo na kufanya agano
mbele ya Yahwe, kutembea pamoja na Yahwe na kukumbuka maagizo yake, kanuni
zake, na sheria zake, kwa moyo wake wote na kwa roho yake yote, kuthibitisha
maneno ya hili agano ambalo lililokuwa limeandikwa kwenye hiki kitabu. Hivyo
watu wote wakakubaliana kusimama kwenye agano 4 Mfalme akamwamuru Hilkia
yule kuhani mkuu, makuhani chini yake, na walinzi wa lango watoe kwenye hekalu
vyombo vilivyokuwa vimetengenezwa kwa ajili ya Baali na Ashera, na kwa ajili
ya nyota zote za mbinguni. Akivichoma moto Yerusalimu kwenye mashamba ya
bonde la Kidroni na kubeba majivu yake kwenda Betheli. 5 Akawaondoa makuhani
waliokuwa wanaabudu miungu ambao wafalme wa Yuda waliwachagua ili kwa
ajili ya kufukiza ubani katika mahali pa juu kwenye miji ya Yuda na sehemu
zinazoizunguka Yerusalemu-wale waliokuwa wanchoma ubani kwa Baali, kwa juana
kwa mwezi, kwa sayari, na kwa nyota zote za mbinguni. 6 Akaiondoa Ashera
kutoka kwenye hekalu la Yahwe, nje ya Yerusalemu hata bonde la Kidroni na
kuichoma hapo. Akaipiga kwenye mavumbi na kuiyatupa yale mavumbi kwenye
makaburi ya watu wa kawaida. 7 Akavisafisha vyumba vya makahaba ambao
walikuwa kwenye hekalu la Yahwe, ambako wanawake waliposhonea nguo kwa
ajili ya Ashera 8 Yosia akawaleta makuhani wote nje ya miji ya Yuda na kupanajisi
mahali pa juu ambako makuhani walipokuwa wakichomea ubani, kutoka Geba hata
Bersheba. Akapaharibu mahala pa juu kwenye malango ambayo yaliyokuwa ya
kuingilia kwenda kwenye lango la Yoshua (liwali wa mji), upande wa kushoto wa
lango la mji. 9 Ingawa makuhani wa mahali pa juu hawakuruhusiwa kuhudumu
kwenye madhabahu ya Yahwe katika Yerusalemu, wakala mikate isiyotiwa chachu
miongoni mwa ndugu zao. 10 Yosia akainajisi Tofethi, ambayo ipo kwenye bonde
la Ben Hinomu, ili kwamba mtu yeyote asimuweke mtoto wake wa kiume au
binti yake kwenye moto kama sadaka kwa Molaki. 11 Akawachukua farasi ambao
wafalme wa Yuda waliokuwa wametolewa kwa ajili ya jua. Walikuwa kwenye
eneo la lango la uingilia kwenye hekalu la Yahwe, karibu na chumba cha Nathani
Meleki, msimamizi mkuu wa nyumba ya mfalme. Yosia akayachoma yale magari
ya farasi ya jua 12 Yosia mfalme akayaharibu madhabahu yaliyokuwa kwenye dari
ya juu ya chumba cha Ahazi, ambacho wafalme wa Yuda walikitengeneza, na
madhabahu ambayo Manase aliyatengeneza kwenye behewa mbili za nyumba ya
Yahwe. Yosia akazivunga vipande vipande na kuvitupa kwenye bonde la Kidroni.
13 Mfalme akapaangamiza mahali pa juu magharibi mwa Yerusalemu, kusini mwa
mlima wa uharibifu ambapo Sulemani mfalme wa Israeli alipajenga kwa ajili ya
Ashtorithi, chukizo la Wamoabu; sanamu za karaha za Wasidoni; kwa Kemoshi,
sanamu za karaha wa Moabu; na kwa Moleki, sanamu wa karaha wa watu wa Amoni.
14 Akazivunja nguzo za jiwe kuwa vipande vipande na kuziangusha chini nguzo
za Ashera na kuzijaza zile sehemu kwa mifupa ya watu. 15 Yosia pia akaiteketeza
kabisa madhabahu iliyokuwa Betheli na mahali pa juu ambako Yeroboamu mwana
wa Nebati (ambaye aliwafanya Waisraeli kuasi) aliijenga. Pia aliichoma moto ile

madhabahu na mahali pa juu na kupapiga hadi pakawa vumbi. Pia akaichoma
moto nguzo ya Ashera. 16 Yosia alipotazama kwenye lile eneo, akagundua kwamba
yale makaburi yalikuwa juu ya mlima. Akawatuma watu kuichukua mifupa kutoka
kwenye yale makaburi; kisha akaichoma kwenye madhabahu, akainajisi. Hii
ilitokana na neno la Yahwe ambalo mtu wa Mungu aliliongea, yule mtu aliyekuwa
ameongea haya mambo kabla. 17 Kisha akasema, "Ni ukumbusho wa nani ule
ninao uona?" Mtu wa ule mji akamwambia, "Lile ni kaburi la mtu wa Mungu
ambaye alikuja kutoka Yuda na kuongea kuhusu haya mambo ambayo ameyafanya
dhidi ya madhabahu ya Betheli." 18 Hivyo Yosia akasema, "Mwacheni. Mtu
asihamishe mifupa yake." Hivyo wakaacha mifupa yake, pamoja na mifupa ya
nabii ambaye alikuja kutoka Samaria. 19 Kisha Yosia akahamisha nyumba zote za
mahali pa juu ambazo zilikuwa katika mji wa Samaria, ambazo wafalme wa Israeli
walizokuwa wamezitengeneza, na ambazo zilizokuwa zimemgadhabisha Yahwe kwa
hasira. 20 Aliwafanyia kile ambacho kilikuwa kimefanyika katika Betheli. Aliwachinja
makuhani wote wa mahali pa juu ya madhabahu na aliichoma mifupa ya watu
juu yao. Kisha akarudi Yerusalemu. 21 Kisha mfalme akawaamuru watu wote,
akisema, "Itunzeni Pasaka ya Yahwe Mungu wenu, kama ilivyoandikwa kwenye
hiki kitabu cha agano." 22 Hiyo Pasaka haijawahi kufanyika tangu siku za waamuzi
ambao waliiongoza Israeli, wala katika siku zote za wafalme wa Israeli au Yuda.
23 Lakini katika mwaka wa kumi na nane wa Mfalme Yosia hii Pasaka ya Yahwe
ilisheherekewa katika Yerusalemu. 24 Yosia pia akawafukuza wale ambao waliokuwa
wameongea na wafu au na roho. Pia aliifukuza miungu ya sananmu, sanamu, na
vitu vyote ambavyo ni chukizo vilivyokuwa vinaonekana katika nchi ya Yuda na
katika Yerusalemu, hivyo kwa kuthibitisha yale maneno ya sheria ambayo iliyokuwa
imeandikwa kwenye kitabu cha Hilkia yule kuhani aliyekuwa amepatikana kwenye
nyumba ya Yahwe. 25 Kabla ya Yosia, hapakuwa na mfalme kama yeye, aliyekuwa
amemwelekea yahwe kwa moyo wake wote, roho yake yote, na nguvu zake zote,
ambaye alifuata sheria zote za Musa. Hapakuwa na mfalme kama Yosia aliyeinuka
baada ya yeye. 26 Walakini, Yahwe hakugeuka kutoka kwenye ukali wa hasira yake,
ambayo ilikuwa dhidi ya Yuda kwa waabudu wapagani wote pamoja ambao Manase
aliokuwa amemgadhibisha. 27 Hivyo Yahwe akasema, "Pia nitaiondoa Yuda usoni
kwangu, kama nilivyoiondoa Israeli, na nitautupilia mbali huu mji ambao nilio
uchagua, Yerusalemu, na ile nyumba ambayo niliyokuwa nimesema, 'Jina langu
litakuwa humo."' 28 Kama kwa mambo mengine yanayo muhusu Yosia, kila kitu
alichofanya, je vimeandikwa kwenye kitabu cha matukio ya wafalme wa Yuda?
29 Katika siku zake, Farao Neko, mfalme wa Misri, alienda kupigana dhidi ya mfalme
wa Ashuru huko mto Frati. Mfalme Yosia akaenda kuonana na Neco katika mapigano,
na Neko akamuua huko Megido. 30 Watumishi wa Yosia wakambeba kwenye gari la
farasi akiwa amekufa kutoka Migido, kumleta Yerusalemu, na kumzika katika kaburi
lake mwenyewe. Kisha watu wa nchi wakamchukua Yehoahazi mwana wa Yosia,
wakamtia mafuta, na kumfanya kuwa mfalme katika mahali pake. 31 Yehoahazi
alikuwa na umri wa miaka ishirini na tatu alipoanza kutawala, na alitawala miezi
mitatu katika Yerusalemu. Mama yake alikuwa akiitwa Hamutali; alikuwa binti wa
Yeremia wa Libana. 32 Yehoahazi alifanya yaliyo maovu usoni kwa Yahwe, kama kila
kitu ambacho babu zake walichokifanya. 33 Farao Neko akamfunga gerezani huko
Ribla katika nchi ya Hamathi, hivyo asiweze kutawala katika Yerusalemu. Kisha
Neko akaitoza Yuda talanta mia moja za fedha na talanta moja ya dhahabu. 34 Farao
Neko akamfanya Eliakimu mwana wa Yosia mfalme katika mahali pa Yosia baba yake,
na kubadilisha jina lake kuwa Yehoyakimu. Lakini akamchukua mfalme Yehoahazi
kwenda Misri, na Yehoahazi akafia huko. 35 Yehoyakimu akalipa fedha na dhahabu

kwa Farao. Ili akutane na amri ya Farao, Yehoyakimu akaitoza nchi na kulazimisha
kila mtu miongoni mwa watu wa nchi wamlipe fedha na dhahabu kulingana na
makadirio yao. 36 Yehoyakimu alikuwa na umri wa miaka ishirini na tano alipoanza
kutawala, na alitawala miaka kumi na moja katika Yerusalemu. Mama yake alikuwa
akiitwa Zebida; alikuwa binti wa Pedaia wa Ruma. 37 Yehoyakimu akafanya yale
yaliyo maovu usoni kwa Yahwe, kama waliyoyafanya babu zake.

# 24

1 Katika siku za Yehoyakimu, Nebukadreza mfalme wa Babeli akaiteka Yuda;
Yehoyakimu akawa mtumishi kwa muda wa miaka mitatu. Kisha Yehoyakimu
akarudi na kuasi dhidi ya Nebukadreza. 2 Yahwe akatuma vikosi vya Wakaldayo
dhidi ya Yehoyakimu,, Washami, Wamoabu, na Waamoni; akawatuma dhidi ya Yuda
kuiharibu. Hii ilikuwa ni kuthibitisha pamoja na neno la Yahwe ambalo aliloliongea
kupitia watumishi wake manabii. 3 Ilikuwa baada ya mda mfupi kwenye kinywa cha
Yahwe kwamba hili likaja juu ya Yuda, kuwaondoa usoni mwa uso wake, kwa sabau
ya dhambi za Manase, yote aliyoyafanya, 4 na pia kwa sababu ya damu isiyokuwa
na hatia aliyoimwaga, kwa kuijaza Yerusalemu kwa damu isiyokuwa na hatia.
Yahwe hakuwa tayari kusamehe hilo. 5 Kama kwa mambo mengine yanayomuhusu
Yehoyakimu, na yote aliyoyafanya, je hayajaandikwa kwenye kitabu cha matukio
ya wafalme wa Yuda? 6 Yehoyakimu akalala pamoja na wazee wake, na Yekonia
mtoto wake akawa mfalme katika sehemu yake. 7 Mfalme wa Misri hakushambulia
tena nje ya nchi yake, kwa sababu mfalme wa Babeli alakuwa amezishinda nchi
zote ambazo zilikuwa zikitawaliwa na mfalme wa Misri, kutoka kwenye kitabu cha
Misri mpaka Mto wa Frati. 8 Yekonia alikuwa na umri wa miaka kumi na nane
alipoanza kutawala; alitawala Yerusalemu miezi mitatu. Mama yake alikuwa anaitwa
Nehushta; alikuwa binti wa Elnathani wa Yerusalemu. 9 Alifanya yaliyo maovu usoni
mwa Yahwe; alifanya yale yote ambayo baba yake aliyafanya. 10 Katika kipindi hicho
jeshi la Nebukadreza mfalme wa Babeli liliishambulia Yerusalemu na kuuzunguka
mji. 11 Nebukadreza mfalme wa Babeli akaja kwenye mji wakati maaskari wake
walipokuwa wameuzunguka, 12 na Yekonia mfalme wa Yuda akatoka nje kwenda
kwa mfalme wa Babeli, yeye, mama yake, watumishi wake, watoto wake, na maafisa
wake. Mfalme wa Babeli akamteka katika mwaka wa nane wa utawala wake.
13 Nebukadreza akachukua kutoka pale vitu vyote vya thamani katika nyumba ya
Yahwe, na walio katika nyumba ya kifalme. Akavikata vipande vipande vitu vyote
vya dhahabu ambavyo Suleimani mfalme wa Israeli alivitengeneza katika hekalu
la Yahwe, kama alivyokuwa amesema ingetokea. 14 Akawachukua wote utumwani
Yerusalemu, viongozi wote, na wapiganaji wote, mateka elfu kumi, na mafundi
wote, na wafua vyuma. hakuna aliyekuwa amesalia isipokuwa watu maskini katika
nchi. 15 Nebukadreza akamchukua Yekonia utumwani Babeli, pia na mama yake na
mfalme, wake, maafisa, na wakuu wa nchi. Akawachukua kwenda utumwani kutoka
Yerusalemu mpaka Babeli. 16 Wapiganaji wote, elfu saba kwa hesabu, na mafundi
elfu moja na wafua vyuma, wote wanaostahili kumpiga- mfalme wa Babeli aliwaleta
hawa watu kwenye utumwa Babeli. 17 Mfalme wa Babeli akamfanya Matania, kaka
yake na baba yake na Yehokimu, mfalme katika sehemu yake, na kubadilisha jina
lake kuwa Sedekia. 18 Sedekia alikuwa na umri wa miaka ishirini na moja wakati
alipoanza kutawala; alitawala miaka kumi na moja katika Yerusalemu. Mama yake
alikuwa anaitwa Hamutali; alikuwa binti wa Yeremia kutoka Libna. 19 Alifanya yaliyo
maovu machoni mwa Yahwe; aliyafanya yale yote ambayo Yehokimu aliyoyafanya.
20 Kupitia hasira ya Yahwe, haya matukio yote yalitokea Yerusalemu na Yuda, hadi
alipowaondoa kwenye uso wake. Kisha Sedekia akaasi dhidi ya mfalme wa Babeli.

# 25

[1] Ilitokea kwamba katika mwaka wa tisa wa utawala wa mfalme Sedekia, katika
mwezi wa kumi, na siku ya kumi ya huo mwezi, Nebukadreza mfalme wa Babeli
alikuja pamoja na jeshi lake lote kwa ajili ya kupigana dhidi ya Yerusalemu.
Akaweka kambi kuelekeana nayo, na wakajenga ukuta kuizunguka. [2] Hivyo mji
huo ulizungukwa mpaka miaka kumi na moja ya utawala wa Sedekia. [3] Katika
siku ya tisa ya mwezi wa nne wa huo mwaka, njaa ilikuwa kali sana kwenye huo
mji kwamba hapakuwa na chakula kwa ajili ya watu wa nchi. [4] Wakati huo ule
mji ulikuwa umebomoka ndani, na wapiganaji wote wakakimbia usiku kwa njia ya
lango kati ya kuta mbili, karibu na bustani ya mfalme, ingawa Wakaldayo walikuwa
wote wameuzunguka mji. Mfalme akaenda kuelekea upande wa Araba. [5] Lakini
jeshi la Wakaldayo likamfuata mfalme Sedekia na kumchukua katika tambarare ya
bonde la Mto Yoradani karibu na Yeriko. Jeshi lake lote lilitawanyika wakamwacha.
[6] Wakamkamata mfalme na kumleta mpaka kwa mfalme wa Babeli huko Ribla,
ambapo walipitisha hukumu juu yake. [7] Kama kwa watoto wa Sedekia, wakawachinja
mbele ya macho yake. Kisha akamtoa macho Sedekia, wakamfunga pingu, na
kumpeleka hadi Babeli. [8] Basi katika mwezi wa tano, katika siku ya saba ya
mwezi, ambapo ulikuwa mwaka wa kumi na tisa wa utawala wa Nebukadreza
mfalme wa Babeli, Nebuzaradani, mtumishi wa mfalme wa Babeli na amrijeshi
wa walinzi wake, wakaja hadi Yerusalemu. [9] Akaichoma moto nyumba ya Yahwe,
nyumba ya mfalme, na nyumba zote za Yeruselemu; pia kila jengo la muhimu
katika mji akayachoma. [10] Kama kwa kuta zote zilizoizunguka Yerusalemu, jeshi
lote la Wababeli ambao walikuwa chini ya amrishi wa walinzi wakaziharibu.
[11] Basi watu waliokuwa wamebaki ambao walikuwa wameondoka katika mji, wale
waliokuwa wameasi kwa mfalme wa Babeli, na mabaki ya watu-Nebuzadani, amiri
jeshi wa mlinzi, wakachukuliwa kwenda utumwani. [12] Lakini amiri jeshi wa
mlinzi aliwaacha baadhi ya maskini wa nchi ili wafanye kazi kwenye shamba la
mizabibu na kulima. [13] Na zile nguzo za shaba ambazo zilikuwa kwenye nyumba
ya Yahwe, na misimamio na bahari ya chuma ambayo ilikuwa kwenye nyumba
ya Yahwe, Wakaldayo wakazivunja vipande vipande na kubeba shaba kuirudisha
Babeli. [14] Masufuria, mabeleshi, makasi, vijiko, na vyombo vyote vya shaba ambavyo
kuhani alivyokuwa amevitunza kwenye hekalu-Wakaldayo wakavichukua vyote.
[15] Masufuria ya kuhamisha majivu na mabakuli ambayo yalikuwa yametengenezwa
kwa dhahabu, na yale yaliyotengenezwa kwa fedha-yule nahodha wa mlinzi wa
mfalme akavichukua pia. [16] Zile nguzo mbili, ile bahari, na vile vitako ambavyo
Suleimani alivitengeneza kwa ajili ya nyumba ya Yahwe shaba ya vyombo hivyo vyote
haikuwa na uzani. [17] Urefu wa ile nguzo ya kwanza ulikuwa ridhaa kumi na nane,
na kichwa cha shaba kilikuwa juu yake. Na urefu wa kichwa ulikuwa ridhaa tatu,
pamoja na mapambo ya wavu na makomamanga yote yakizunguka kwenye hicho
kichwa, vyote vilikuwa vimetengenezwa kwa shaba. Na ile nguzo nyingine ilikuwa
vivyo hivyo kama ile ya kwanza pamoja na wavu wake. [18] Yule amiri jeshi wa mlinzi
akamchukua Seraya kuhani mkuu, pamoja za Sefania, yule kuhani wa pili, na walinzi
watatu wa kwenye lango. [19] Kutoka mjini akamchukua mlinzi, afisa mmoja ambaye
aliyekuwa msimamizi wa maaskari, na watu watano ambao walikuwa wakimshauri
mfalme, ambao walikuwa bado katika mji. Pia alimchukua mfungwa wa afisa jeshi
la mfalme, kwa ajili ya kuandika watu kwenye jeshi, pamoja na watu sitini muhimu
kutoka hiyo nchi ambao walikuwa katika mji. [20] Kisha Nebuzaradani, amiri wa
mlinzi, akawachukua na kuwapeleka kwa mfalme Babeli huko Ribla. [21] Mfalme wa
Babeli akawaua huko Ribla katika nchi ya Hamathi. Kwa njia hii, Yuda akaiacha nchi
yake kwenda utumwani. [22] Na wale watu waliokuwa wamebakia katika nchi ya Yuda,

wale ambao Nebukadreza mfalme wa Babeli aliwaacha, akamuweka Gedalia mwana
wa Ahikamu, mwana wa Shafani, msimamizi wao. [23] Kisha wakati maamiri wote
wa majeshi, wao na watu wao, waliposikia kwamba mfalme wa Babeli amemfanya
Gedalia kuwa liwali, wakaenda kwa Gedalia huko Mispa. Hawa watu walikuwa
Ishmaeli mwana wa Nethania, Yohanani mwana wa Karea, Seraya mwana wa
Tanhumethi Mnetofa, na Yezania mwana wa Mmaaka-wao na watu wao. [24] Gedalia
akafanya kiapo kwa watu wake na kuwaambia, “Msiwaogope Wakaldayo. Muishi
katika nchi na kumtumikia mfalme wa Babeli, na itakuwa vema kwenu.” [25] Lakini
ilitokea kwamba katika mwezi wa saba Ishmaeli mwana wa Nethania mwana wa
Elishama, kutoka familia ya kifalme, wakaja na watu kumi na kumshambulia Gedalia.
Gedalia akafa, pamoja na watu wa Yuda na Wababeli ambao walikuwa pamoja nae
huko Mizpa. [26] Kisha wale watu wote, kutoka chini kwenda juu, na maamiri wa
jeshi, wakainuka na kwenda Misri, kwasababu walikuwa wanawaogopa Wababeli.
[27] Ilitokea baadaye katika mwaka wa thelathini na saba wa utumwa wa Yekonia
mfalme wa Yuda, katika mwezi wa kumi na mbili, siku ya ishirini na saba ya mwezi,
Evil-merodaki mfalme wa Babeli akamtoa Yekonia mfalme wa Yuda kutoka gerezani.
Hii ilitokea katika mwaka ambao Evil-Merodaki alipoanza kutawala. [28] Akaongea
naye kwa ukarimu na kumpatia kiti kizuri zaidi kuliko kile cha wafalme wengine
ambao walikuwa pamoja naye Babeli. [29] Evil-Merodaki akamvua Yekonia nguo za
gerezani, [30] na Yekinia akala siku zote kwenye meza ya mfalme katika maisha yake
yote yaliyokuwa yamebakia.

# 1 Mambo ya Nyakati

1 Adamu, Sethi, Enoshi, 2 Kenani, Mahalaleli, Yaredi, 3 Henoko, Methusela, Lameki.
4 Wana wa Nuhu walikuwa ni Shemu, Hamu, na Yafethi. 5 Wana wa Yafethi
walikuwa ni Gomeri, Magogu, Madai, Yavani, Tubali, Mesheki, na Tirasi. 6 Wana
wa Gomeri walikuwa Ashkenazi, Rifathi na Togama. 7 Wana wa Yavani walikuwa ni
Elisha, Tarshishi, Kitimu, na Warodani. 8 Wana wa Hamu walikuwa ni Kushi, Misri,
Putu, na Kanaani. 9 Wana wa Kushi walikuwa ni Seba, Havila, Sabta, Raama, na
Sabteka. Wana wa Raama walikuwa ni Sheba na Dedani. 10 Kushi akawa baba wa
Nimrodi, aliyekuwa shujaa wa Kwanza katika dunia. 11 Misri akawa babu wa Waludi,
Waanami, Walehabi, Wanaftuhi, 12 Wapathrusi, Wakasluhi (Wafilisti walipotoka),
na Wakaftori. 13 Kanaani akawa baba wa Sidoni, mwanae wa kwanza, na wa
Hethi. 14 Pia akawa babu wa Myebusi, Mwamori, Mgirgashi, 15 Mhivi, Mwarki,
Msini, 16 Mwarvadi, Msemari, na Mhamathi. 17 Wana wa Shemu walikuwa Elamu,
Ashuru, Arfaksadi, Ludi, Aramu, Usi, Huli, Getheri, na Mashi. 18 Arfaksadi akawa
baba wa Sala, na Sala akawa baba wa Eberi. 19 Eberi alikuwa na wana wawili
wa kiume. Jina la wa kwanza lilikuwa Pelegi, kwa kuwa katika siku zake dunia
ilikuwa imegawanyika. Jina la kaka yake lilikuwa Yoktani. 20 Yoktani akawa baba
wa Almodadi, Shelefu, Hasarmawethi, Yera, 21 Hadoramu, Uzali, Dikla, 22 Obali,
Abimaeli, Sheba, 23 Ofiri, Havila, na Yobabu; wote hawa walikuwa uzao wa Yoktani.
24 Shemu, Arfaksadi, Sala, 25 Eberi, Pelegi, Reu, 26 Serugi, Nahori, Tera, 27 Abramu,
aliye kuwa Ibrahimu. 28 Wana wa Ibrahimu walikuwa Isaka na Ishmaeli. 29 Hawa
ndio wanao: mzaliwa wa kwanza alikuwa ni Nebayothi, kisha Kedari, Abdeeli,
Mibsamu, 30 Mishma, Duma, Masa, Hadadi, Tema, 31 Yeturi, Nafishi, na Kedama.
Hawa ndio wana wa Ishamaeli. 32 Wana wa Ketura, suria wa Ibrahimu, walikuwa
Zimrani, Yokshani, Medani, Midiani, Ishbaki, na Shua. Wana wa Yokshani walikuwa
Sheba na Dedani. 33 Wana wa Midiani walikuwa Efa, Eferi, Hanoki, Abida, na Eldaa.
Wote hawa walikuwa uzaowa Ketura. 34 Ibrahimu akawa baba wa Isaka. Wana wa
Isaka walikuwa Esau na Israeli. 35 Wana wa Esau walikuwa ni Elifazi, Reueli, Yeushi,
Yalamu, na Kora. 36 Wana wa Elifazi walikuwa ni Temani, Omari, Sefo, Gatamu,
Kenazi, Timna, na Amaleki. 37 Wana wa Reueli walikuwa ni Nahathi, Zera, Shama,
na Miza. 38 Wana wa Seiri walikuwa ni Lotani, Shobali, Sebioni, Ana, Dishoni, Eseri,
na Dishani. 39 Wana wa Lotani walikuwa ni Hori na Hemamu, na Timna alikuwa
dada yake Lotani. 40 Wana wa Shobali walikuwa ni Alvani, Manahathi, Ebali, Shefo,
na Onamu. Wana wa Sebeoni walikuwa ni Aya na Ana. 41 Mwana wa Ana alikuwa ni
Dishoni. Wana wa Dishoni walikuwa Hemdani, Eshbani, Ithrani, na Kerani. 42 Wana
wa Eseri walikuwa Bilhani, Zaawani, na Akani. Wana wa Dishani walikuwa Usi na
Arani. 43 Hawa ndio wafalme walio tawala katika nchi ya Edomu kabla ya mfalme
yeyote kuwatawala Waisraeli: Bela mwana wa Beori; na jina la mji wake ulikuwa
Dinhaba. 44 Bela alipo kufa, Yohabu mwana wa Zera wa Bosra akatawala badala
yake. 45 Yohabu alipo kufa, Hushamu wa nchi ya Watemani akatawala badala yake.
46 Hushamu alipo kufa, Hadadi mwana wa Bedadi, aliye washinda Wamidiani katika
uwanja wa Moabu, akatawa badala yake. Jina la mji wake ulikuwa Avithi. 47 Hadadi
alipo kufa, Samla wa Masreka akatawala badala yake. 48 Samla alipo kufa, Shauli wa
Rehobothi Hanahari akatawala badala yake. 49 Shauli alipo kufa, Baal-Hanani mwana
wa Akbori akatawala badala yake. 50 Baal-Hanani mwana wa Akbori alipo kufa,
Hadari akatawala badala yake. Jina la mji wake ni Pau. Jina la mke wake lilikuwa
ni Mehetabeli binti wa Matredi binti wa Mezahabu. 51 Hadadi akafa. Wajumbe wa
ukoo wa Edomu walikuwa Timna, Alva, Yethethi, 52 Oholibama, Ela, Pinoni, 53 Kenazi,

Temani, Mibsari, 54 Magdieli, na Iramu. Hawa ndio walikuwa wajumbe wa ukoo wa
Edomu.

# 2

1 Hawa ndio wana wa Israeli: Reubeni, Simioni, Lawi, Yuda, Isakari, Zebuloni,
2 Dani, Yusufu, Benyamini, Naftali, Gadi, na Asheri. 3 Wana wa Yuda walikuwa Eri,
Onani, na Shela, ambao walizaliwa na binti wa Shua, Wakanaani. Eri, mzaliwa wa
kwanza wa Yuda, alikuwa muovu katika macho ya Yahweh, na Yahweh akamwua.
4 Tamari, mkwe wake, alimzalia Peresi na Zera. Yuda alikuwa na wana wa kiume
wa tano. 5 Wana wa Peresi walikuwa Hesroni na Hamuli. 6 Wana wa Zera walikuwa
Zimri, Ethani, Hemani, Kalikoli na Darda, wote kwa jumla ni watano. 7 Mwana wa
Karmi alikuwa ni Akani, aliye leta taabu katika Israeli alipo iba kile kilicho hifadhiwa
kwa ajili ya Mungu. 8 Mwana wa Ethani alikuwa Azaria. 9 Wana wa Hezroni
walikuwa ni Yerameeli, Ramu, na Kalebu. 10 Ramu akawa baba wa Aminadabu, na
Aminadabu akawa baba wa Nashoni, kiongozi miongoni uzao wa Yuda. 11 Nashoni
akawa baba wa Salmoni, na Salmon akawa baba wa Boazi. 12 Boazi akawa baba wa
Obedi, na Obedi akawa baba wa Yese. 13 Yese akawa baba wa mzaliwa wake wa
kwanza Eliabu, wa pili Abinadabu, wa tatu Shama. 14 Nethaneli wa nne, Radai wa
tano. 15 Ozemu wa sita, na Daudi wa saba. 16 Dada zao walikuwa Seruya na Abigaili.
Wana wa Seruya walikuwa Abishai, Yoabu, na Asaheli, jumla watatu. 17 Abigali
akamzaa Amasa, ambaye baba yake alikuwa Yetheri Mwishmaeli. 18 Kalebu mwana
wa Hesroni akawa baba wa watoto wa Azubu mkewe, na Yeriothi. Wanawe walikuwa
Yesheri, Shobabu, na Ardoni. 19 Azuba akafa, na Kalebu akamuoa Efrathi, aliye mzalia
Huri. 20 Huri akawa baba wa Uri, na Uri akawa baba wa Besaleli. 21 Baadae Hesroni
(alipo kuwa na miaka sitini) akamuoa binti wa Makiri, baba wa Gileadi. Akamzalia
Segubu. 22 Segubu akawa baba wa Yairi, aliye miliki miji ishirini na mitatu katika
nchi ya Gileadi. 23 Geshuri na Aramu wakawapokonya miji ya Yairi na Kenathi,
pamoja na miji sitini iliyo zunguka. Hawa wakazi wote walikuwa ni uzao wa Makiri,
baba wa Gileadi. 24 Baada ya kifo cha Hesroni, Kalebu akalala na Efrata, mke wa
baba yake Hesroni. Akamzalia Ashuri, baba wa Tekoa. 25 Wana wa Yerameeli,
mzaliwa wa kwanza wa Hesroni, walikuwa ni Ramu mzaliwa wa kwanza, Buna,
Oreni, Ozemu, na Ahiya. 26 Yerameeli alikuwa na mke mwingine, Jina lake lilikuwa
Atara. Yeye alikuwa mama wa Onamu. 27 Wana wa Ramu, mzaliwa wa kwanza
wa Yerameeli, walikuwa Maasi, Yamini, na Ekeri. 28 Wana wa Onamu walikuwa
ni Shamai na Yada. Wana wa Shamai walikuwa ni Nadabu na Abishuri. 29 Jina
la mke wa Abishuri lilikuwa Abihaili, na akamzalia Abani na Molidi. 30 Wana wa
Nadabu walikuwa Seledi na Apaimu, lakini Seledi alikufa pasipo watoto. 31 Mwana
wa Apaimu alikuwa Ishi. Mwana wa Ishi alikuwa Sheshani. Mwana wa Sheshani
alikuwa Alai. 32 Wana wa Yada, kaka yake Shamai, walikuwa Yetheri na Yonathani.
Yetheri alikufa pasipo mtoto. 33 Wana wa Yonathani walikuwa Pelethi na Zaza. Hawa
ndio uzao wa Yerameeli. 34 Sasa Sheshani hakuwa na watoto wa kiume, bali wa
kike pekee. Sheshani alikuwa na mtumishi, wa Kimisri, ambaye jina lake lilikuwa
Yariha. 35 Sheshani alimkabidhi binti yake kwa Yariha mtumishi wake kama mke
wake. Akamzalia Atai. 36 Atai akawa baba wa Nathani, na Nathani akawa baba wa
Zabadi. 37 Zabadi akawa baba wa Efalali, na Afalali akawa baba wa Obedi. 38 Obedi
akawa baba wa Yehu, na Yehu akawa baba wa Azaria. 39 Azaria akawa baba wa
Helesi, na Helesi akawa baba wa Eleasa. 40 Eleasa akawa baba wa Sismai, na Sismai
akawa baba wa Shalumu. 41 Shalumu akawa baba wa Yekamia, na Yekamia akawa
baba wa Elishama. 42 Wana wa Kalebu, kaka yake Yerameeli, walikuwa ni Mesha
mzaliwa wake wa kwanza, aliye kuwa baba wa Zifu. Mwanae wa pili, Maresha,
allikuwa baba wa Hebroni. 43 Wana wa Hebroni walikuwa Kora, Tapua, Rekemu,

na Shema. 44 Shema akawa baba wa Rahamu, baba wa Yorkeamu. Rekemu akawa
baba wa Shamai. 45 Mwana wa Shamai alikuwa Maoni, na Maoni alikuwa baba wa
Bethsuri. 46 Efa, suria wa Kalebu, alimza Harani, Mosa, na Gazezi. Harani akawa baba
wa Gazezi. 47 Wana wa Yadai walikuwa Regemu, Yothamu, Geshani, Peleti, Efa, na
Shaafa. 48 Maaka, suria wa Kalebu, alimza Sheberi na Tirhana. 49 Pia akamza Shaafu
baba wa Madmana, Sheva baba wa Makbena na baba wa Gibea. Binti wa Kalebu
alikuwa Aksa. Hawa walikuwa uzao wa Kalebu. 50 Hawa walikuwa wana wa Huri,
mzaliwa wake wa kwanza kwa Efratha: Shobali baba wa Kiriath-Yearimu. 51 Salma
baba wa Bethlehemu, na Harefu baba wa Beth-gaderi. 52 Shobali baba wa kiriath-
Yearimu alikuwa na uzao: Haroe, nusu ya watu Wamenuthite, 53 na ukoo wa Kiriath-
Yearimu: Waithri, Waputhi, Washumathi, na Wamishrai. Wasorathi na Waeshtaoli
walitoka huku. 54 Ukoo wa Salma ulikuwa kama ufatao: Bethlehemu, Wanetofathi,
Atroth-Beth-Yoabu, na nusu ya Wamenuhothi na Wazori, 55 ukoo wa waandishi walio
ishi Yabesi: Watirathi, Washimeathi, na Wasukathi. Hawa walikuwa Wakeni walio
toka katika uzao wa Hamathi, babu wa Warekabu.

# 3

1 Sasa hawa ndio wana wa Daudi waliozaliwa kwake huko Hebroni: mzaliwa wa
kwanza alikuwa Amnoni, kwa Ahinoamu kutoka Yezreeli; wa pili alikuwa Danieli,
kwa Abigaili kutoka Karmeli; 2 watatu alikuwa Absalomu, ambaye mama yake
alikuwa ni Maaka, binti wa Talmai mfalme wa Geshuri. Wanne alikuwa ni Adoniya
mwana wa Hagithi; 3 watano alikuwa ni Shefatia kwa Abitali, wasita alikuwa ni
Ithraeamu kwa Egla mkewe. 4 Hawa sita walizaliwa kwa Daudi huko Hebroni,
alipo tawala miaka saba na miezi sita. Kisha akatawala miaka thelathini na mitatu
huko Yerusalemu. 5 Hawa wana wa nne, kwa Bathshua binti wa Amieli, walizaliwa
kwake huko Yerusalemu: Shamua, Nathani, na Sulemani. 6 Wana tisa wengine wa
Daudi walikuwa ni: Ibhari, Elishua, Elipeleti, 7 Noga, Nefegi, Yafia, 8 Elishama, na
Elifeleti. 9 Hawa walikuwa wana wa Daudi, pasipo kuwehesababu wana wa masuria
wake. Tamari alikuwa dada yao. 10 Mwana wa Sulemani alikuwa ni Rehoboamu.
Mwana wa Rehoboamu alikuwa Abiya. Mwana wa Abiya alikuwa Asa. Mwana
wa Asa alikuwa Yehoshafati. 11 Mwana wa Yehoshafati alikuwa Yoramu. Mwana
wa Yoramu alikuwa Ahazia. Mwana wa Ahazia alikuwa Yoashi. 12 Mwana wa
Yoashi alikuwa Amazia. Mwana wa Amazia alikuwa Azaria. Mwana wa Azaria
alikuwa Yothamu. 13 Mwana wa Yothamu alikuwa Ahazi. Mwana wa Ahazi alikuwa
Hezekia. Mwana wa Hezekia alikuwa Manase. 14 Mwana wa Manase alikuwa Amoni.
Mwana wa Amoni alikuwa Yosia. 15 Wana wa Yosia aliyekuwa mzaliwa wake wa
kwanza ni Yohana, wapili Yehoyakimu, mwanae watatu Sedekia, na mwanae wanne
Shalumu. 16 Wana wa Yehoyakimu walikuwa Yehoyakini na Sedekia. 17 Wana wa
YehoYakini, mateka, walikuwa Shealtieli, 18 Malkiramu, Pedaya, Shenezari, Yekamia,
Hoshama, na Nedabia. 19 Wana wa Pedaya walikuwa Zerubabeli na Shimei. Wana
wa Zerubabeli walikuwa Meshulamu na Hanania; Shelomithi alikuwa dada yao.
20 Wanae watano walikuwa Hashuba, Oheli, Berekia, Hasadia, na Yushabu Hesedi.
21 Wana wa Hanania walikuwa Pelatia na Yeshaya. Mwanawe alikuwa Refaya, na
uzao wake zaidi walikuwa ni Arnani, Obadia, na Shekania. 22 Mwana wa Shekania
alikuwa Shemaya. Wana wa Shemaya walikuwa Hatushi, Igali, Baria, Nearia, na
Shafati. 23 Wana watatu wa Nearia walikuwa Elioenai, Hizekia, na Azrikamu. 24 Wana
saba wa Elioenai walikuwa Hodavia, Eliashibu, Pelaya, Akubu, Yohana, Delaya, na
Anani.

# 4

1 Uzao wa Yuda ulikuwa Peresi, Hesroni, Karmi, Huri, na Shobali. 2 Shobali
alikuwa baba wa Reaya. Reaya alikuwa baba wa Yahathi. Yahathi alikuwa baba
wa Ahumai na Lahadi. Hawa walikuwa mababu wa koo za Wasorathi. 3 Hawa

walikuwa mababu wa ukoo katika mji wa Etamu: Yezreeli, Ishma, na Idbashi. Babu
yao alikuwa Haselelponi. 4 Penueli alikuwa babu wa koo katika mji wa Gedori. Ezeri
alikuwa muanzilishi wa koo katika Husha. Hawa walikuwa uzao wa Huri, mzaliwa
wa kwanza wa Efrathi na muanzilishi wa Bethelehemu. 5 Ashuri baba wa Tekoa
alikuwa na wake wawili, Hela na Naara. 6 Naara alimzalia Ahuzamu, Heferi, Temeni
na Ahashtari. Hawa walikua wana wa Naara. 7 Wana wa Hela walikua Serethi,
Ishari, Ethnani, 8 na Kozi, alikua baba wa Anubu na Sobeba, na koo zilizotoka kwa
Aharheli mwana wa Harumu. 9 Yabesi aliheshimika zaidi ya kaka zake. Mama yake
alimuita Yabesi. Alisema, "Kwasababu nimemzaa katika huzuni." 10 Yabesi akamuita
Mungu wa Israeli na kusema, "Kama tu utanibariki mimi, ongeza mipaka yangu, na
mkono wako ukuwa juu yangu. Ukifanya hivi utaninusuru na mabaya, ili kwamba
niwe huru na huzuni!" Kwa hivyo Mungu akamjalia maombi yake. 11 Kelubu kaka
wa Shuha akawa baba wa Mehiri, aliyekuwa baba wa Eshtoni. 12 Eshtoni akawa
baba wa Beth-Rafa, Pasea, na Tehina, ambaye alianzisha mji wa Nahashi. Hawa ni
wanaume walioishi Reka. 13 Wana wa Kenazi walikua Othinieli na Seraia. Wana wa
Othinieli walikuwa Hathathi na Meonothai. 14 Meonothai akawa baba wa Ofara, na
Seraia akawa baba wa Yohabu, mwanzilishi wa Ge Harashimu, ambao watu wake
walikua wahunzi. 15 Wana wa Kalebu mwana wa Yefune walikua Iru, Ele na Namu.
Wana wa Ela alikua Kenazi. 16 Wana wa Yehaleli walikua Zifi, Zifa, Tiriya, na Azareli.
17 Wana wa Ezra walikua Yetheri, Meredi, Eferi, na Yaloni. 18 Mke wake Meredi wa
Kimisri alimzalia Miriamu, Shamai, na Ishibahi, aliyekua baba wa Eshitemoa. Hawa
walikua wana wa Bithia, binti wa Farao, ambaye Meredi alimuoa. Mke wa Kiyahudi
wa Meredi alimzalia Yeredi, ambaye alikua baba wa Gedore; Heberi, aliyekua baba
wa Soko; na Yekuthieli aliyekua baba wa Zanoa. 19 Kati ya watoto wawili wa mke
wa Hodia, dada wa Nahamu, mmoja wao kawa baba wa Keila Mgarimite. Mwingine
alikua Eshitemoa Mmakathite. 20 Wana wa Shimoni walikua Amnoni, Rina, Beni
Hanani, na Tilon. Wana wa Ishi walikua Zohethi na Beni Zoheti. 21 Uzao wa Shela
mwana wa Yuda, Ulikua ni Eri baba wa Leka, Laada baba wa Maresha na koo
za wafanyakazi wa kushona kule Beth Ashbea, 22 Yoakimu, Wanaume wa Kozeba,
na Yoashi na Sarafi, waliokua na mali huko Moabu, lakini walirudi Bethlehemu.
( Maelezo haya yametoka kwenye nakala za zamani.) 23 Baadhi ya watu hawa
walikuwa ni wafinyanzi walioishi Netaimu na Gedera na wakawa wafanyakazi wa
Mfalme. 24 Uzao wa Simeoni ulikua Jamini, Jaribu, Zera, na Shauli. 25 Shalumu
alikua mwana wa Shauli, Mibisamu mwana wa Shalumu, na Mishima mwana wa
Mibisamu. 26 Ukoo wa Mishima ulikua Hamueli mwana wake, Zakuri mjukuu wake,
na Shimei kitukuu chake. 27 Shimei alikua na wana kumi na sita na mabinti sita. Kaka
yake hakua na watoto wengi, Hivyo koo zao hazikuongezeka kwa idadi kubwa kama
wato wa Yuda walivyoongezeka. 28 Waliishi Beasheba, Molada, na Hazari Shuali.
29 Pia waliishi Bilha, Ezemu, Toladi, 30 Bethueli, Horma, Zikilagi, 31 Bethi Markabothi,
Hazari Susimi, Bethi Biri, na Shaaraimu. Hii ilikua miji yao mpaka utawala wa Daudi.
32 Vijiji vyao vitano vilikua Etamu, Aini, Tocheni, na Ashani, 33 pamoja na mipaka ya
vijiji kwa umbali wa Baali. Haya yalikua makazi yao, na walitunza kumbukumbu
za uzao wao. 34 Viongozi wa ukoo walikua Meshobabu, Yamileki, Yoshahi mwana
wa Amazia, 35 Yoeli, Yehu mwana wa Yoshibia mwana wa Seraia mwana wa Asieli,
36 Elioenai, Yaakoba, Yeshohaia, Asaia, Adieli, Yesimieli, Benaia, 37 na Ziza mwana wa
Shifi mwana wa Aloni mwana wa Yedaia mwana wa Shimiri mwana wa Shemaia.
38 Hawa walio orodheshwa kwa majina walikua viongozi wa koo zao, na koo zao
ziliongezeka sana. 39 Walienda karibu na Gedori, mashariki mwa bonde, kutafuta
malisho ya mifugo yao. 40 Walipata malisho mengi na mazuri. Nchi ilikua tambarare,
tulivu na ya amani. Wahamu waliishi hapo awali. 41 Hao walio orodheshwa hapo
kwa majina walikuja katika siku za Hezekia mfalme wa Yuda, na wakashambulia
makazi ya Wahamu na Wameuni, ambao pia walikua hapo. Waliwaangamiza kabisa

na kuishi hapo sababu walipata malisho kwa ajili ya mifugo yao. 42 Wanaume mia
tano wa kabila la Simeoni walienda katika mlima Seiri, na viongozi wao Pelatia,
Nearia, Refaia, na Uzieli, wana wa Ishi. 43 Waliwashinda wakimbizi wa Waamaleki
waliobakia, na wakaishi hapo hadi siku hii.

# 5

1 Wana wa Rubeni mzaliwa wa kwanza wa Israeli - sasa Rubeni alikuwa mzaliwa
wa kwanza wa Israeli, lakini haki yake ya mzaliwa wa kwanza ilipewa kwa wana
wa Yusufu mwana wa Israeli kwa sababu Rubeni alinajisi kochi la baba yake. Hivyo
hajanakiliwa kama mwana wa kwanza. 2 Yuda alikuwa mwenye nguvu kuliko kaka
zake, na kiongozi ata toka kwake. Lakini haki ya mzaliwa wa kwanza ilikuwa
ya Yusufu - 3 wana wa Rubeni, mzaliwa wa kwanza wa Israeli alikuwa Hanoki,
Palu, Hezroni, na Karmi. 4 Uzao wa Yoeli ulikuwa huu: Mwana wa Yoeli alikuwa
Shemaia. Mwana wa Shemaia alikuwa Gogi. Mwana wa Gogi alikuwa Shimei.
5 Mwana wa Shimei alikuwa Mika. Mwana wa Mika alikuwa Reaia. Mwana wa
Reaia alikuwa Baali. 6 Mwana wa Baali alikuwa Bera, ambaye Tiligathi Pileseri
alimpeleka matekani kule Assiria. Bera alikuwa kiongozi katika kabila la Rubeni.
7 Ndugu wa Bera kwa makabila yao ni hawa wafuatao, wameorodheshwa katika
nakala za uzao wao: Yeieli wa kwanza, Zekaria, na 8 Bela mwana wa Azazi mwana
wa Shema mwana wa Yoeli. Waliishi Aroeri, kwa umbali wa Nebo na Baali Meoni,
9 na mwanzo wa mashariki mwa jangwa lenye umbali wa hadi Mto Efarati. Hii ni
kwa sababu walikuwa na mifugo mingi katika nchi ya Gileadi. 10 Katika siku za
Sauli, kabila la Rubeni lilishambulia Wahagiri na kuwa shinda. Wakaishi ndani ya
hema za Wahagiri katika nchi yote mashariki mwa Gileadi. 11 Kabila la Gadi liliishi
karibu nao, katika nchi ya Bashani umbali wa Saleka. 12 Viongozi wao walikuwa
Yoeli, aliyekuwa kichwa wa ukoo, na Shafamu alikuwa kichwa wa ukoo mwingine,
na Yanai na Shafati walikuwa wa Bashani. 13 Ndugu zao, kwa familia za baba yao,
walikuwa Mikaeli, Meshulamu, Sheba, Yorai, Yakani, na Eberi - jumla saba wote.
14 Hawa watu walio tajwa hapo juu ni uzao wa Abihaili, na Abihaili alikuwa mwana
wa Huri. Huri alikuwa mwana w a Yaroa. Yaroa alikuwa mwana wa Gileadi. Gileadi
alikuwa mwana wa Mikaeli. Mikaeli alikuwa mwana wa Yeshishai. Yeshishai alikuwa
mwana wa Yado. Yado alikuwa mwana wa Buzi. 15 Ahi mwana wa Abidieli mwana
wa Guni, alikuwa kichwa cha familia ya baba yake. 16 Waliishi Gileadi, Bashani,
katika miji, na katika nchi zote za malisho ya Sharoni kwa umbali wa mipaka
yake. 17 Hawa wote waliorodheshwa katika nakaka za uzao katika siku za Yothamu
mfalme wa Yuda na Yeroboamu mfalme wa Israeli. 18 Warubeni, Wagadi, na nusu
ya kabila la Manase walikuwa na wana jeshi elfu arobaini na nne walio fuzu kwa
vita, walio beba ngao na upanga, na pinde na mishale. 19 Waliwashambulia Wahagri,
Yeturi, Nafishi, na Nodabu. 20 Walipokea msaada wa Kimungu dhidi yao. Katika
hili Wahagri na wote walio kuwa nao walishindwa. Hii ni kwa sababu Waisraeli
walipaza sauti katika vita, na yeye akawajibu, kwa sababu waliweka tumaini lao
kwake. 21 Walikamata wanya wao, pamoja na ngamia elfu hamsini, kondoo 250,
000, punda elfu mbili, na wanaume 100, 000. 22 Kwa sababu Mungu aliwapigania,
waliua maadui wengi. Waliishi katika nchi yao mpaka mateka. 23 Baadhi ya watu wa
kabila la Manase waliishi katika nchi ya Bashani kwa umbali wa Hermoni na Seniri
(hiyo ni, Mlima Hermoni). 24 Hawa walikuwa viongozi wa familia zao: Eferi, Ishi,
Elieli, Azrieli, Yeremia, Hodavia, na Yahdieli. Walikuwa wenye nguvu na wanaume
wa jasiri, wanaume maharufu, viongozi wa familia zao. 25 Lakini walikuwa sio wa
aminifu kwa Mungu wa babu zao. Badala yake, waliabudu miungu ya watu waio
nchi, ambao Mungu aliwaangamiza mbele yao. 26 Mungu wa Israeli alimchochea
Puli mfalme wa Assiria ( ambaye pia uitwa Tiligathi Pileseri, mfalme wa Assiria).

Aliwa peleka matekani Warubeni, Wagadi, na nusu ya kabila la Manase. Aliwaleta
kwa Hala, Habori, Hara, na kwenye mto wa Gozani, ambapo wapo adi leo.

# 6

1 Wana wa Levi walikuwa Gerishoni, Kohathi, na Merari. 2 Wana wa Kohathi
walikuwa Amramu, Izhari, Hebroni, na Uzieli. 3 Wana wa Amramu walikuwa Aruni,
Musa, Miriamu. Wana wa Aruni walikuwa Nadabu, Abihu, Eleazari, na Ithamari.
4 Eleazari akawa baba wa Finehasi, na Finehasi akawa baba wa Abishua. 5 Abishua
akawa baba wa Buki, na Buki akawa baba wa Uzi. 6 Uzi akawa baba wa Zerahia,
na Zerahia akawa baba wa Meraioti. 7 Meraioti akawa baba wa Amaria, na Amaria
akawa baba wa Ahitubi. 8 Ahitubi akawa baba wa Zadoki, na Zadoki akawa baba
wa Ahimazi. 9 Ahimazi akawa baba wa Azaria, na Azaria akawa baba wa Yohanani.
10 Yohanani akawa baba wa Azaria, aliye hudumu katika hekalu alilo lijenga Sulemani
ndaniya Yerusalemu. 11 Azaria akawa baba wa Amaria, na Amaria akawa baba wa
Ahitubi. 12 Ahitubi akawa baba wa Zadoki, na Zadoki akawa baba wa Shalumu.
13 Shalumu akawa baba wa Hilikia, na Hilikia akawa baba wa Azaria. 14 Azaria
akawa baba Seraia, na Seraia akawa baba wa Yehozadaki. 15 Yehozadaki akaenda
matekani Yahweh alipo wapeleka utumwani Yuda na Yerusalemu kwa mkono wa
Nebukadneza. 16 Wana wa Levi walikuwa Gerishomu, Kohathi, na Merari. 17 Wana
wa Gerishomu walikuwa Libini na Shimei. 18 Wana wa Kohathi walikuwa Amramu,
Izhari, Hebroni, na Uzieli. 19 Wana wa Merari walikuwa Mahili na Mushi. Hawa
walikuwa koo za Walawi kwa familia za baba zao. 20 Uzao wa Gerishomu ulianza
na mwanae Libini. Mwana wa Libini alikuwa Jahathi. Mwanae alikuwa Zima.
21 Mwanae alikuwa Yoa. Mwanae alikuwa alikuwa Ido. Mwanae alikuwa Zera.
Mwanae alikuwa Yeatherai. 22 Uzao wa Kohathi ulianza na mwanae Aminadabu.
Mwanae alikuwa Kora. Mwanae alikuwa Asiri. 23 Mwanae alikuwa Elikana. Mwanae
alikuwa Ebiasa. Mwanae alikuwa Asiri. 24 Mwanae alikuwa Tahathi. Mwanae
alikuwa Urieli. Mwanae alikuwa uzia. Mwanae alikuwa Shauli. 25 Wana wa Elikana
walikuwa Amasai, Ahimothi, na Elikana. 26 Mwana wa huyu Elikana wa pili alikuwa
Zofai. Mwanae alikuwa Nahathi. 27 Mwanae alikuwa Eliabu. Mwanae alikuwa
Yehoramu. Mwanae alikuwa Elikana. 28 Wana wa Samwali walikuwa mzaliwa wa
kwanza, Yoeli, na Abija, wa pili. 29 Mwana wa Merari alikuwa Mahili. Mwanae
alikuwa Libini. 30 Mwanae alikuwa Shimei. Mwanae alikuwa Uza. Mwanae alikuwa
Shimea. Mwanae alikuwa Hagia. Mwana alikuwa Asaia. 31 Haya ndio majina ya
wanaume ambao Daudi waliwaeka kusimamia muziki katika nyumba ya Yahweh,
baada ya sanduku kuja hapo. 32 Walitumika kwa kuimba mbele ya hema, hema la
kukutania, mpaka Sulemani alipo jenga nyumba ya Yahweh ndani ya Yerusalemu.
Walikamilisha wajibu wao kwa kadiri ya maelekezo waliopewa. 33 Hawa walitumika
pamoja na wana wao. Katika makabila ya Wakohathi alitoka Hemani mwana muziki.
Babu zake walikuwa hawa, kurudi nyuma ya wakati: Hemani alikuwa mwana wa
Yoeli. Yoeli alikuwa mwana wa Samweli. 34 Samweli alikuwa mwana wa Elikana.
Elikana alikuwa mwana wa Yerohamu. Yerohamu alikuwa mwana wa Elieli. Elieli
alikuwa mwana wa Toa. 35 Toa alikuwa mwana wa Zufi. Zufi alikuwa mwana
wa Elikana. Elikana alikuwa mwana wa Mahathi. Mahathi alikuwa mwana wa
Amasai. Amasai alikuwa mwana wa Elikana. 36 Elikana alikuwa mwana wa Yoeli.
Yoeli alikuwa mwana wa Azaria. Azaria alikuwa mwana wa Zefania. 37 Zefania
alikuwa mwana wa Tahathi. Tahathi alikuwa mwana wa Asiri. Asiri alikuwa mwana
wa Ebiasa. Ebiasa alikuwa mwana wa Kora. 38 Kora alikuwa mwana wa Izhari.
Izhari alikuwa mwana wa Kohathi. Kohathi alikuwa mwana wa Levi. Levi alikuwa
mwana wa Israeli. 39 Msaidizi wa Hemani alikuwa Asafu, aliye simama mkono wake
wa kuume. Asafu alikuwa mwana Berekia. Berekia alikuwa mwana wa Shimea.
40 Shimea alikuwa mwana Mikaeli. Mikaeli alikuwa mwana wa Baaseia. Baaseia
alikuwa mwana wa Malikiya. 41 Malikiya alikuwa mwana wa Ethini. Ethini alikuwa
mwana wa Zera. Zera alikuwa mwana wa Adaia. 42 Adaia alikuwa mwana wa Ethani.
Ethani alikuwa mwana wa Zima. Zima alikuwa mwana wa Shimei. 43 Shimei alikuwa

mwana wa Yahathi. Yahathi alikuwa mwana wa Gerishomu. Gerishomu alikuwa
mwana wa Levi. 44 Upande wa mkono wa koshoto wa Hemani walikuwa wasaidizi
wake wana wa Merari. Alikuwa Ethani mwana wa Kishi. Kishi alikuwa mwana wa
Abdi. Abdi alikuwa mwana wa Maluki. 45 Maluki alikuwa mwana wa Hashabia.
Hashabia alikuwa mwana wa Amazia. Amazia alikuwa mwana wa Hilikia. 46 Hilikia
alikuwa mwana wa Amzi. Amzi alikuwa mwana wa Bani. Bani alikuwa mwana wa
Shemeri. 47 Shemeri alikuwa mwana wa Mahili. Mahili alikuwa mwana wa Mushi.
Mushi alikuwa mwana wa Merari. Merari alikuwa mwana wa Levi. 48 Walawi,
alipangiwa kufanya kazi zote za hema, nyumba ya Mungu. 49 Aruni na wana wake
walitoa sadaka katika madhabahu kwa ajili ya sadaka za kuteketeza; na sadaka katika
madhabahu ya uvumba kwa kazi zote katika pa patakatifu. Hizi sadaka zilifanya
maombezi kwa ajili ya Waisraeli, kwa kadiri ya yote ambayo Musa mtumishi wa
Mungu aliwaamuru. 50 Uzao wa Aruni una kumbukwa kama ifuatavyo: Mwana
wa Aruni alikuwa Eleazari. Mwana Eleazari alikuwa Finehasi. Mwana wa Finehasi
alikuwa Abishua. 51 Mwana wa Abishua alikuwa Buki. Mwana wa Buki alikuwa Uzi.
Mwana wa Buki alikuwa Zerahia. 52 Mwana wa Zerahia alikuwa Meraiothi. Mwana
wa Meraiothi alikuwa Amaria. Mwana wa Amaria alikuwa Ahitubi. 53 Mwana wa
Ahitubi alikuwa Zadoki. Mwana wa Zadoki alikuwa Ahimazi. 54 Hizi ni sehemu
ambazo wazao wa Aruni walipangiwa kuishi, wazao wa Aruni ambao walitoka
katika koo za Wakohathi (maeneo ya kwanza yalikuwa yao). 55 Walipewa Hebroni
katika nchi ya Yuda na nchi ya malisho, 56 lakini maeneo ya mji na vijiji alipewa
Kalebu mwana wa Yefune. 57 Kwa wazao wa Aruni waliwapa: Hebroni ( mji wa
makimblio), na Libina pamoja na nchi ya malisho, Yatiri, Eshitemoa pamoja na nchi
ya malisho, 58 Hileni pamoja na nchi ya malisho, na Debiri pamoja na nchi ya malisho.
59 Waliwapa uzao wa Aruni: Ashani pamoja na nchi ya malisho na Bethi Shemeshi
pamoja na nchi ya malisho; 60 na kutoka katika kabila la Benjamini walipewa Geba
pamoja na nchi ya malisho, Alemethi pamoja na nchi ya malisho, na Anothothi na
nchi ya malisho. Jumla ya miji yao ilikuwa kumi na tatu. 61 Uzao mwengine wa
Kohathi waliwapa kwa sehemu miji kumi kutoka kwa kabila la Manase. 62 Kwa uzao
wa Gerishomu kwa koo zao tofauti walipewa miji kumi na tatu kutoka kwa makabila
ya Isakari, Asheri, Naftali, na nusu ya kabila la Manase huko Bashani. 63 Kwa uzao wa
Merari walipewa miji kumi, kulingana na koo zao, kutoka kwa makabila ya Rubeni,
Gadi, na Zebuluni. 64 Hivyo watu wa Israeli walitoa hii miji pamoja na nchi za
malisho kwa Walawi. 65 Walitoa kwa sehemu miji iliyo tajwa awali kutoka katika
kabila la Yuda, Simeoni, na Benjamini. 66 Kwa baadhi ya koo za Wakohathi walitoa
miji kutoka kwa kabila la Efraimu. 67 Waliwapa: Shekemu ( mji wa makimbilio)
pamoja na nchi ya malisho katika milima ya Efraimu, Gezeri na nchi ya malisho,
68 Jokimeamu pamoja na nchi ya malisho, Bethi Horoni pamoja na nchi ya malisho,
69 Aiyaloni pamoja na nchi ya malisho, na Gathi Rimoni pamoja na nchi ya malisho.
70 Nusu ya kabila la Manase waliwapa Wakohathi: Aneri pamoja na nchi ya malisho
na Bileamu pamoja na nchi ya malisho. Hizi zikawa mali za koo za Wakohathi. 71 Kwa
uzao wa Gerishomu kutoka koo za nusu ya kabila la Manase, waliwapa: Golani huko
Baashani na nchi ya malisho na Ashitarothi pamoja na nchi ya malisho. 72 Kabila
la Isakari liliwapa uzao wa Gerishomu: Kedeshi pamoja na nchi ya malisho, Dabera
pamoja na nchi ya malisho, 73 Ramothi pamoja na nchi ya malisho, na Anemu pamoja
na nchi ya malisho. 74 Isakari alipokea kutoka kwa kabila la Asheri: Mashali pamoja
na nchi ya malisho, Abdoni pamoja na nchi ya malisho, 75 Hukoki pamoja na nchi
ya malisho, na Rehobu pamoja na nchi ya malisho. 76 Walipokea kutoka kabila la
Naftali: Kedeshi iliyo Galileya pamoja na nchi ya malisho, Hamoni pamoja na nchi
ya malisho, na Kiriathaimu pamoja na nchi ya malisho. 77 Kwa Walawi wengine, uzao
wa Merari, walipewa kutoka kabila la Zebuluni: Rimono pamoja na nchi ya malisho
na Tabori pamoja na nchi ya malisho. 78-79 Kwa wao pia walipewa, upande wa pili

wa Yordani huko Yeriko, kwa upande wa mashariki mwa mto: Bezeri katika jangwa
pamoja na nchi ya malisho, Yahzahi pamoja na nchi ya malisho, Kedemothi pamoka
na nchi ya malisho, ma Mefathi pamoja na nchi ya malisho. Hizi zilitolewa kutoka
kabila la Rubeni. 80 Walawi walipokea kutoka kabila la Gadi: Ramothi ya Gileadi
pamoja na nchi ya malisho, Mahanaimu pamoja na nchi ya malisho, 81 Heshiboni
pamoja na nchi ya malisho, na Yazeri pamoja na nchi ya malisho.

# 7

1 Isiakari alikuwa na wana wanne Tola, Pua, Yashubi, na Shimironi. 2 Wana wa
Tola walikuwa Uzi, Refaia, Yerie, Yamai, Ibisami, Shemueli. Walikua vichwa katika
nyumba za baba yao, toka uzao wa Tola na waliorodheshwa kama mashujaa hodari
miongoni mwa kizazi chao. Katika siku za Daudi walikua na idadi ya 22, 600.
3 Mwana wa Uzi alikua Izrahia. Mwana wake alikua Michaeli, Obadia, Yoeli, na Ishia,
wote watano walikua viongozi wa ukoo 4 Pamoja nao walikua na jeshi la watu elfu
thelathini na sita kwa mapambano, Kwa mujibu wa orodha zilizomilikiwa na koo za
mababu zao, kwa kuwa walikuwa na wake wengi pamoja na wana. 5 Kaka zao, kabila
la Isakari, walikua na wanaume wa vita themanini na saba, kwa mujibu wa orodha
zilizomilikiwa na koo za mababu zao. 6 Wana watatu wa Benjamini walikuwa Bela,
Beka, na Yediaeli. 7 Wana watano wa Bela walikuwa Ezibono, Uzi, Uzieli, Yerimoti,
na Iri. Walikua ni wanajeshi na waanzilishi wa koo. Watu wao walikuwa na idadi ya
wanaume wa vita 22, 034, kwa mujibu wa orodha zilizomilikiwa na koo za mababu
zao. 8 Wana wa Beka walikuwa Zemira, Yoashi, Elieza, Elionai, Omri, Yeremoti,
Abiya, Anatoti, na Alemeti. Wote hawa walikuwa wana wake. 9 Orodha ya koo
zao ilikua na idadi ya 20, 200 viongozi wa familia na wanaume wa vita. 10 Mwana
wa Yediaeli alikuwa Bilhani. Wana wa Bilhani walikuwa Yeushi, Benjamini, Ehudi,
Kenaana, Zetani, Tarishishi, na Ahishahari. 11 Wote hawa waikuwa wana wa Yediaeli.
Waliorodheshwa katika ukoo orodha ilikuwa 17, 200 viongozi na wanaume wa vita
imara kwa kazi ya jeshi. 12 (Shupimu na Hupimu walikuwa wana wa Iri, na Hushimu
alikuwa mwana wa Aheri.) 13 Wana wa Naftali walikuwa Yazieli, Guni, Yezeri, na
Shalumu. Hawa walikuwa wajukuu wa Bilhahi. 14 Manasse alikua na mtoto wa kiume
aliitwa Asrieli, Ambaye suria wake wa Kiaramia alimzalia. Pia alimzaa na Makiri,
baba wa Gileadi. 15 Makiri alimchukua mke wake kutoka Hupite na Shupite. Jina
la dada yake lilikuwa Maaka. Mwingine wa uzao wa Manasse alikuwa Zalofehadi,
ambaye alikuwa na mabinti pekee. 16 Maaka mke wa Makiri, alimzaa mwana na
alimuita Pereshi. Kaka yake aliitwa Shereshi, na wana wake walikuwa Ulamu na
Rakemu. 17 Mwana wa Ulami alikuwa Bedani. Hawa walikuwa uzao wa Gileadi
mwana wa Makiri mwana wa Manase. 18 Dada wa Gileadi Hamoleketi alimzaa
Ishihodi, Abi Ezeri, na Mahila. 19 Wana wa Shemida walikuwa Ahiana, Shekemu,
Liki, na Aniamu. 20 Uzao wa Efraimu ulikuwa kama ifuatavyo: Efraimu mwana wa
Shutela. Shutela mwana wa Beredi. Beredi mwana wa Tahati. 21 Tahati mwana wa
Eleada. Eleada mwana wa Shutela. (Eza na Eleadi waliuawa na wanaume wa Gati,
wenyeji wa nchi, walipoenda kuiba mifugo yao. 22 Efraimu baba yao aliomboleza
kwa siku nyingi, na kaka zake walikuja kumfariji. 23 Alilala na mkewe. Akapata
mimba akamzaa mwana. Efraimu akamuita Beria, kwa sababu maafa yalishakuja
nyumbani mwake. 24 Binti yake alikuwa Sheera, ambaye alijenga miji juu na chini
Beth Horon na Uzzen Sheerah.) 25 Mwana wake alikuwa Rafa. Mwana wa Rafa
alikuwa Reshefi. Mwana wa Reshafi alikuwa Tela. Mwana wa Tela alikuwa Tahani.
26 Mwana wa Tahani alikuwa Ladani. Mwana wa Ladani alikuwa Amihudi. Mwana
wa Amihudi alikuwa Elishama. 27 Mwana wa Elishama alikuwa Nuni. Mwana wa
Nuni alikuwa Joshua. 28 Mali zao na makazi yao yalikuwa Betheli na yalizungukwa na
vijiji. Waliongeza upande wa mashariki hadi Naarani na upande wa magharibi hadi
Gezeri na vijiji vyake, na Shekemu na vijiji vyake hadi Aya na vijiji vyake. 29 Katika

mipaka pamoja na Manasse kulikuwa na Beti shani na vijiji vyake, Taanaki na vijiji
vyake, Megido na vijiji vyake, na Dori na vijiji vyake. Katika huu mji waliishi uzao
wa Josefu mwana wa Israeli. 30 Wana wa Asha walikuwa Imna, Ishiva, Ishivi, na
Beria. Sera alikuwa dada yao. 31 Wana wa Beria walikuwa Heberi na Malchieli,
Ambaye alikuwa baba wa Birzaiti. 32 Wana wa Heberi walikuwa Yafeti, Shomer, na
Hotamu. dada yao alikuwa Shua. 33 Wana wa Yafeti walikuwa Pasach, Bimhali, na
Ashivati. hawa walikuwa watoto wa yafeti. 34 shoma, kaka wa Yafeti alikuwa na wana
hawa: Roga, Yehuba, Aram. 35 Kaka yake Shema, Helemu, alikuwa na wana hawa:
Zofa, Imna, Sheleshi na Amali. 36 Wana wa Zofa walikuwa Sua, Harinefa, Shua, Beri,
IMra, 37 Beza, Hodi, Shamma, Shilsha, Ithrani, na Beera. 38 Wana wa Yeta walikuwa
Jefune, Pispa, na Ara. 39 Wana wa Ulla walikwa Ara, Hannieli, na Rizia. 40 Hawa wote
walikuwa uzao wa Asha. Walikua mababu wa ukoo, viongozi wa familia, wananume
wa kipekee, wanaume wa vita, na machifu kati ya viongozi. Kulikuwa na wanaume
elfu ishirini na sita walioorodheshwa waliokuwa imara kwa kazi ya jeshi, kwa mujibu
wa idadi iliyo orodheshwa.

# 8

1 Wana watano wa Benjamini walikuwa Bela mwana wake wa kwanza, Asibeli,
Ahara, 2 Noha, na Rafa. 3 Wana wa Bela walikuwa Adari, Gera, Abihudi, 4 Abishau,
Naamani, Ahoa, 5 Gera, Shefufani, na Huramu. 6 Hawa walikuwa uzao wa Ehudi
ambao walikuwa vichwa vya koo kwa wakazi wa Geba, ambao walihimizwa kuhamia
Manahati: 7 Naamani, Ahijahi, na Gera. Wa mwishi, Gera, aliwaongoza katika
kuhama. Alikuwa baba wa Uza na Ahihudi. 8 Shaharaimu akawa baba wa watoto
katika ardhi ya Moabu, baada ya kuwatariki wake zake Hushimu na Baara. 9 kwa
mke wake Hodeshi, Shaharaimu akawa baba wa Yobabu, Zibia, Mesha, Malkamu,
10 Yeuzi, Shachia, na Mirima. Hawa walikuwa wana wake, viongozi katika koo zao.
11 Alikwisha kuwa baba wa Abitubi, na Elipaali kwa Hushimu. 12 Wana wa Elipaali
walikuwa Eba, Mishamu, na Shemedi ( ambao walijenga Ono na Lod pamoja na
vijiji vilivyozunguka.) 13 Pia walikuwako Beria na Shema. Walikuwa vichwa vya
koo walizoishi Aijalon, Ambao waliwaondoa wakazi wa Gati. 14 Beria alikuwa na
wana watatu: Ahio, Shashaki, Jeremothi, 15 Zebadia, Aradi, Eda, 16 Mikaeli, Ishipa,
na Joha. 17-18 Elipaa alikuwa na wana hawa: Zebadia, Meshulamu, Hiziki, Heba,
Ishimerai, Izilia, na Yobabu. 19 Shimei alikuwa na wana hawa: Yokimu, Zikri, Zabdi,
20 Elienai, Zilletai, Elieli, 21 Adaia, Beraia, na Shimrati. 22 Shashaki alikuwa na wana
hawa: Ishipani, Eba, Elieli, 23 Abdoni, Zikri, Hanani, 24 Hanania, Elamu, Antotoja,
25 Ifdeia, na Penueli. 26 Yerohamu alikuwa na wana hawa: Shamsherai, Sheharia,
Atli, 27 Yaareshia, Elija, na Zikri. 28 Hawa walikuwa vichwa vya koo na viongozi
walioishi Yerusalemu. 29 Baba wa Gibeoni, Jeieli, ambaye mke wake aliitwa Maaka,
aliishi ndani ya Gibeoni. 30 Uzao wake wa kwanza alikuwa Abdoni, akafatia Zuri,
Kishi, Baali, Nadab, 31 Gedori, Ahio, na Zekari. 32 Mwana mwingine wa Yeieli alikuwa
Mikloti, ambaye akaja kuwa baba wa Shimea. Pia wanaishi karibu na ndugu zao
Yerusalemu. 33 Neri alikuwa baba wa Kishi. Kishi alikuwa baba wa Sauli. Sauli
alikuwa baba wa Yonathani, Malkishua, Abinadabu, na Ishbaali. 34 Mwana wa
Yonathani alikuwa Meribu Baali. Meribu Baali alikuwa baba wa Mika. 35 Wana wa
Mika walikuwa Pithoni, Meleki, Tarea, and Ahazi. 36 Ahazi akawa baba wa Yehoada.
Yehoada alikuwa baba wa Amelethi, Azimavethi, na Zimri. Zimri alikuwa baba wa
Moza. 37 Moza alikuwa baba wa Binea. Binea alikuwa baba wa Rafa. Rafa alikuwa
baba wa Eleasa. Eleasa alikuwa baba wa Azeli. 38 Azeli alikuwa na wana sita:
Azrikamu, Bokeru, Ishimaeli, Obadia, na Hanani. Wote hawa walikuwa wana wa
Azeli. 39 Wana wa Esheki, kaka yake, walikuwa Ulamu mzaliwa wake wa kwanza,
Yeushi wa pili, na Elifeleti wa tatu. 40 Wana wa Ulamu walikuwa wanaume wa

mapambano na warusha mishale wa zuri. Walikuwa na wana wengi na wajukuu,
jumla ya 150. Wote hawa walikuwa uzao wa Benjamini.

# 9

1 Kwa hivyo watu wote wa Israeli walinakiliwa ki uzao. Walinakiliwa katika vitabu
vya kifalme vya Israeli. Yuda, walipelekwa matekani Babylon kwasababu ya dhambi
zao. 2 Wakwanza kurudi kuishi katika miiji yao walikuwa Waisraeli, Makuhani,
Walawi, na Watumishi wa hekalu. 3 Baadhi ya uzao wa Yuda, Benjamin, Efraimu, na
Manase waliishi Yerusalemu. 4 Wahamiaji walijumusha Uthai mwana wa Ammihudi
mwana wa Omri mwana wa Bani, moja ya uzao wa Perezi mwana wa Yuda. 5 Kati
ya Mashilonite kulikuwa na Asaia mtoto wa kwanza na wana wake. 6 Kati ya uzao
wa Zera alikuwa Yeuli. Uzao wao ulikuwa na namba 690. 7 Katika uzao Benjamini
walikuwa Salu mwana wa Meshulamu mwana wa hodavia mwana wa Hssenua. 8 Pia
walikuwa Ibneia mwana wa Yerohamu; Ela mwana wa Uzzi mwana wa Mikri; na
Meshullam mwana wa Shefatia mwana waReuli mwana wa Ibnija. 9 Ndugu zao
waliandika kwenye orodha ya namba 956 ya vizazi vyao. Wanaume wote hawa
walikuwa viongozi wa koo za mababu zao. 10 Makuhani walikuwa Yedaia, Yehoiarib,
na Yokini. 11 Walikuwa pia Azaria mwana wa Hilkia mwana wa Meshullamu mwana
wa Zadoki mwana wa Meraioti mwana wa Ahitubi, aliyekuwa na mamlaka katika
nyumba ya Mungu. 12 Kulikuwa na Adaia mwana wa Yerohamu mwana wa Pashuri
mwana wa Malkija. Pia kulikuwa na Maasai mwanawa Adieli mwana wa Yazera
mwana wa Meshulamu mwana wa Meshilemiti mwana wa Imma. 13 Ndugu zao,
ambao walikuwa viongozi katika koo za mababu zao, idadi ya 1, 760. Walikuwa ni
wanaume wenye uwezo sana wa kufanya kazi katika nyumba ya Mungu. 14 Kati ya
Walawii, kulikuwa na Shemaia mwana wa Hashubu mwana wa Azrikam mwana wa
Hashabia, kati ya uzao wa Merari. 15 Walikuwako pia Bakbakari, Hereshi, Galali,
na Mattania mwana wa Mika mwana wa Zikri mwana wa Asafu. 16 Walikuwako
pia Obadia mwana wa Shemaia mwana wa Galali mwana wa Yedutuni; na Berekia
mwana wa Asa mwana wa Elkana, aliyeishikatika vijiji vya Netophathites. 17 Walinzi
wa lango walikuwa Shalumu, Akubi, Talimoni, Ahimani, na uzao wao. Shalumu
alikuwa kiongozi wao. 18 Awali walisimama kulinda katika geti la mfalme upande
wa mashariki wa kambi ya uzao wa Walawi. 19 Shalumu mwana wa Kore mwana
wa Ebiasafu, ambaye kama mwana wa Kora, na ndugu zake kutoka nyumba ya baba
yake, Korahite, alikuwa na mamlaka kwa kazi ya huduma, Walilinda mlango wa
hema, kama mababu zao walivyolinda kambi ya Yawehi, na pia walilinda lango
la kuingilia. 20 Finehasi mwana wa Eleaza aliwaongoza kipindi cha nyuma, na
Yahwehi alikuwa pamoja nae. 21 Zekaria mwana wa Meshelemia alikua mlinzi katika
mlango wa kuingilia hekalu, “eneo la kukutania.” 22 Hawa wote walichaguliwa kana
walinzi wa mageti ya kuingilia kwa idadi ya 212. Majina yao yaliandikwa kwenye
kumbukumbu za watu katika vijiji vyao. Mtabiri aliwaweka Daudi na Samueli katika
nafasi ya uaminifu. 23 Kwa hivyo wao na watotot wao walilinda mageti katika
nyumba ya Yawehi, hema la kuabudia. 24 Walinzi wa mageti waliwekwa katika
pande zote nne, upande wa mashariki, magharibi, kaskazini, na kusini. 25 Kaka zao,
walioishi kwenye vijiji vyao, walikuja kuwasaidia baada ya mzunguko wa siku saba.
26 Lakini viongozi wanne wa walinzi, ambao walikwa walawi, walipangiwa kulinda
vyumba na vyumba vya kuhifadhi katika nyumba ya Mungu. 27 Walitumia usiku wao
sehemu walizowekwa kuzunguka nyumba ya Mungu, kwao ilikuwa ni wajibu wao
kulinda. Na walifungua geti kila asubuhi. 28 Baadhi yao waliwajibika katika hekalu
la vifaa; walihesabu makala zilizo ingizwa ndani na zilizo tolewa nje. 29 Baadhi yao
pia waliwekwa kutunza vitu vitakatifu, vifaa, na vitu, kujuisha unga safi, mvinyo,

mafuta, manukato, na uvumba. 30 Baadhi ya wana wa makuhani walichanganya
uvumba. 31 Matithia, mmoja wa walawi, ambaye alikuwa mtoto wa kwanza wa
Shalumu wa Wakorahi, alikuwa na wajibu wa kuandaa mikate kwa ajili ya sadaka.
32 Baadhi ya kaka zao, uzao wa kohathite, waliwajibika kwa mikate ya uwepo,
kuandaa kila Sabatho. 33 Waimbaji na viongozi wa familia ya Walawi waliishi ndani
ya vyumba katika mahali takatifu walipo kuwa hawafanyi kazi, kwa sababu wapiswa
kufanya kazi walio pangiwa usiku na mchana. 34 Hawa walikuwa viongozi wa familia
miongoni mwa Walawi, kama ilivyo orodheshwa katika kumbukumbu za uzao wao.
Waliishi Yerusalemu. 35 Baba wa Gibeoni, Yeiel, ambaye mkewe aliitwa Maaka, aliishi
Gibeoni. 36 Mtoto wake wa kwanza alikuwa Abdoni, alafu wana wake Zuri, Kishi,
Baali, Neri, Nadabu, 37 Gedori, Ahio, Zekaria, na Mikloti. 38 Mikloti alikuwa baba wa
Shimeamu. Pia waliishi karibu na kaka yao huko Yerusalemu. 39 Neri alikuwa baba
wa Kishi. Kishi alikuwa baba wa Sauli. sauli alikuwa baba wa Yonathani, malkishua,
Abinadabu, na Ishbaali. 40 Mwana wa Jonathani alikuwa Merib baali. Merib baali
alikuwa baba wa Mika. 41 Mwana wa Mika walikuwa pithoni, Meleki, Tahrea, na
ahazi. 42 Ahazi alikuwa baba wa Jara. Jara alikuwa baba wa Alemeti, Azmaveti,
na zimri. Zimri alikuwa baba wa Moza. 43 Moza alikuwa baba wa Binea. Binea
alikuwa baba wa Refaia. Refaia alikuwa baba wa Eleas. eleasa alikuwa baba wa
Azeli. 44 Wana sita wa Azeli walikuwa Azrikamu, Bochera, Ishmaeli, shearia, Obdia,
na Hanani. hawa walikuwa wana wa Azeli

# 10

1 Wafilisti wakapigana dhidi ya Israeli. Kila mwanaume wa Israeli alikimbia
Wafilisti na kuanguka na kufa katika Mlima Giliboa. 2 Wafilisti waliwakimbiza Sauli
na mwanae. Waflisti walimuua Yonathani, Abinadabu, na Malichishua, wana wake.
3 Pambano lilikuwa zito kwa Sauli, na wapiga mishale wakamshambulia. Alipatwa
na maumivu makali sababu ya wapiga mishale. 4 Kisha Sauli akasema kwa mbeba
ngao wake, “Vuta upanga wako na unichome nao. Lasihivyo, hawa wasio tahiriwa
watukuja na kunitesa”. Lakini mbeba ngao wake hakutaka, kwa kuwa aliogopa sana.
Kwa hiyo Sauli akachukuwa upanga wake na kuuangukia. 5 Mbeba ngao alivyoona
kuwa Sauli amekufa, naye akaangukia upanga wake na kufa. 6 Kwaiyo Sauli akafa,
na wana wake watatu, wote wa nyumba yake wakafa pamoja. 7 Kila mwanaume wa
Israeli katika bonde alivyoona kuwa wamekimbia, na Sauli na wana wake wamekufa,
walitelekeza miji yao na kukimbia. Kisha Wafilisti wakaja na kuishi humo. 8 Ikawa
siku inayofuata, Wafilisti walipo kuja kukagua wafu, walimkuta Sauli na wana wake
wameanguka katika Mlima Giliboa. 9 Wakamvua nguo zote na kuchukuwa kichwa
chake na ngao yake. Wakatuma wajumbe wapeleke habari Filistia yote kwa miungu
yao na watu wote. 10 Ngao yake wakaeka ndani ya hekalu la miungu yao, na kichwa
chake waka kining'iniza katika hekalu la Dagoni. 11 Yabeshi Gileadi yote ilipo sikia
Wafilisti waliyo mtendea Sauli, 12 wanaume wote wa vita wakaenda na kuchukuwa
mwili wa Sauli na hiyo ya wanae, na kuirejesha Yabeshi. Walizika mifupa yao chini ya
mti huko Yabeshi na wakafunga siku saba. 13 Kwaiyo Sauli akafa kwa kuwa hakuwa
mwaminifu kwa Yahweh. Hakutii maelekezo ya Yahweh, lakini akauliza ushauri kwa
mtu anaye ongea na wafu. 14 Hakutafuta mwongozo kwa Yahweh, hivyo Yahweh
akamua na kupindua ufalme kwa Daudi mwana wa Yese.

# 11

1 Kisha Waisraeli wote walikuja Hebroni kwa Daudi na kusema, “Angalia, sisi ni
nyama na mifupa yako. 2 Katika wakati uliopita, Sauli alipoo kuwa mfalme juu
yetu, ni wewe uliye ongoza jeshi la Israeli. Yahweh Mungu wako alisema kwako,
'utawachunga watu wangu wa Isaraeli, na utakuwa mtawala wa watu wangu wa

Israeli"'. 3 Kwaiyo wazee wote wa Israeli wakamjia mfalme huko Hebroni, na Daudi
akafanya agano nao mbele ya Yahweh. Wakampaka mafuta Daudi kuwa mfalme wa
Israeli. Kwa namna hii, neno la Yahweh lilo nenwa na Samweli likawa kweli. 4 Daudi
na Israeli yote wakaenda Yerusalemu (yani, Yebusi). Sasa Wayebusi, wakazi wa nchi,
walikuwa pale. 5 Wakazi wa yebusi wakamwabia Daudi, "Hautakuja humu." Lakini
Daudi alichukuwa ngome ya Sayuni, mji wa Daudi. 6 Daudi alisema, "Yeyote atakaye
washambulia Wayebusi wa kwanza atakuwa mkuu wa jeshi" kwaiyo Yoabu mwana
wa Zeruia akashambulia wa kwanza, hivyo akafanywa mkuu wa jeshi. 7 Daudi
akaanza kuishi katika hiyo ngome. Kwaiyo wakaiita mji wa Daudi. 8 Akaimarisha mji
kutoka Milo na hadi mpaka ukuta unao zunguka. Yoabu akaimairisha mji wote uliyo
baki. 9 Daudi akawa mkuu na mkuu kwa sababu Yahweh wa Majeshi alikuwa naye.
10 Hawa walikuwa viongozi Daudi aliyo kuwa nao, waliyo jionyesha imara katika
ufalme wake, pamoja na Israeli, kumfanya mfalme, kutii neno la Yahweh kuhusu
Israeli. 11 Hii ni orodha ya wanajeshi shupavu wa Daudi. Yashobeami, mwana wa
Mhakimoni, alikuwa mkuu wa kikosi cha thelathini. Aliwaua wanaume mia tatu na
mkuki wake katika sehemu moja. 12 Baada ya yeye alikuwa Eleazari mwana wa Dodo,
Mahohi, aliyekuwa mmoja wa wanaume watatu hodari. 13 Alikuwa na Daudi huko
Pasidamimu, na pale Wafilisti wakakusanyika pamoja kwa mapambano, ambapo
palikuwa na uwanja wa ngano na jeshi liliwakimbia Wafilisti. 14 Walisimama katikati
ya uwanja. Wakautetea na kuwakata Wafilisti na Yahweh akawaokoa na ushindi
mkubwa. 15 Kisha watatu wa viongozi thelathini wakashuka chini kwenye mwamba
wa Daudi, katika pango la Adulamu. Jeshi la Wafilisti walieka kambi katika bonde la
Refaim. 16 Kwa wakati huo Daudi alikuwa katika ngome yake, pangoni, Wafilisti
walikita kambi yao Bethilehemu. 17 Daudi alikuwa na kiu ya maji na akasema,
"Laiti mtu akanipatia maji ya kunywa kutoka kisima kilicho Bethilehemu, kisima
kilicho pembeni mwa lango!" 18 Hawa wanaume hodari watatu wakatoboa kupita
jeshi la Wafilisti na kuchota maji kwenye kisima cha Bethilehemu, kisima pembeni
mwa lango. Wakachukuwa maji na kumletea Daudi, lakini alikataa kunywa. Badala
yake, akamwaga chini kwa Yahweh. 19 Kisha akasema, "Yahweh, iwe mbali na mimi,
kwamba ni yanywe haya maji. Je ninywe damu ya wanaume walio hatarisha maisha
yao?" Kwa sababu wameeka maisha ya hatarini, akakataa kunywa. Haya ni mambo
wanaume hodari watatu walio fanya. 20 Abishai kaka wa Yoabu, alikuwa kiongozi
wa watatu. Alitumia mkuki wake dhidi ya watu mia tatu na kuwaua. Ametajwa
pamoja na wale watatu. 21 Kati ya wale watatu, yeye alipewa heshima mara mbili
na akawa kiongozi wao. Japo hakuwa mmoja wa miongoni mwao. 22 Benaia mwana
wa Yehoiada alikuwa mwanaume mwenye nguvu aliye fanya mambo makuu. Aliua
wana wawili wa Arieli wa Moabu. Pia alishuka chini ya shimo na kumuua simba
wakati theluji ikianguka. 23 Alimua hadi Mmisri, mwanaume mwenye mita mbili na
theluthi moja. Mmisri alikuwa na mkuki kama gongo la mshonaji, lakini alimfuata
chini na fimbo tu. Akakamata mkuki katika mkono wa Mmisri na kumuua na mkuki
wake. 24 Benaia mwana wa Yehoiada alifanya haya matukio, na akatajwa miongoni
mwa wale wanaume hodari watatu. 25 Alisifika zaidi ya wale wanajeshi thelathini
kwa ujumla, lakini hakuwa pewa hadhi ya wale wanajeshi watatu hodari. Daudi
alimueka kiongozi wa walinzi wake. 26 Wanaume hodari walikuwa Asaheli kaka
wa Yoabu, Elhanani mwana wa Dodo wa Bethilehemu, 27 Shamothi Mherori, Helezi
Mpeloni, 28 Ira mwana wa Ikeshi Mtekoi, Abi Eza Manathothi, 29 Sibekai Mhushathite,
Ilai Mahohite, 30 Maharai Mnetofathi, Heledi mwana wa Baana Mnetofathite, 31 Itai
mwana wa Ribai wa Gibea uzao wa Benjamini, Benaia Mpirathoni, 32 Hurai wa
mabonde ya Gaashi, Abieli Marbathi, 33 Azmavethi Mbaharumi, Eliaba Mshaalboni,
34 Mwana wa Hashemu Mgizoni, Yonathani mwana wa Shagee Mhararite, 35 Ahiamu

mwana wa Sacari Mhararite, Elifali mwana wa Uri, 36 Hefa Mmekarathi, Ahija
Mpeloni, 37 Hezro Mcarmeli, Maarai mwana wa Ezibai, 38 Yoeli kaka wa Nathani,
Mibhari mwana wa Hagiri, 39 Zeleki Mamoni, Naharai Mberothi ( mbeba ngao ya
Yoabu mwana wa Zeruia), 40 Ira Mithire, Garebu Mithire, 41 Uria Mhiti, Zabadi mwana
wa Ahlai, 42 Adina mwana wa Shiza Mreubeni ( kiongozi wa Wareubeni) na thelathini
pamoja nae, 43 Hanani mwana wa Maaka, na Yoshafati Mmithini, 44 Uzia Mashiterathi,
Shama na Yeieli wana wa Hothamu Waaroeri, 45 Jediaeli mwana wa Shimri, Joha (
kaka yake Mtize), 46 Elieli Mmahavi, Yeribai na Yoshavia mwana wa Elnaamu, Ithima
Mmoabi, 47 Elieli, Obedi, na Yaasieli Wamezobai.

# 12

1 Hawa walikuwa wanaume walio kuja kwa Daudi huko Zikilagi, wakati akiwa
bado amefukuzwa katika uwepo wa Sauli mwana wa Kishi. Walikuwa miongoni
mwa wanajeshi, wasaidizi wake katika mapambano. 2 Walikuwa wana upinde na
waliweza kutumia mkono wa kuume na wakushoto kurusha mawe na manati na
kupiga mishale kutoka kwenye upinde. Walikuwa Wabenjamini, ndugu wa kabila
moja na Sauli. 3 Kiongozi alikuwa Ahi Eza, halafu Yoashi, Wana wote wa Shemaa
Mgibeathi. Kulikuwa na Yezieli na Peleti, wana wa Azimavethi. Kulikuwa pia na
Beraka, Yehu Waanathothi, 4 Ishimaia Mgibeoni, mwanajeshi kati ya wale thelathini
( na kiongozi wa wale thelathini); Yeremia, Yahazieli, Yohana, Yozabadi Wagederathi,
5 Eluzai, Yerimothi, Bealia, Shemaria, Shefatia Waharufi, 6 Wakorahi ni Elkana, Ishia,
Azareli, Yoeza, Yashobeamu, na 7 Yoela na Zebadia, wana wa Yeroham wa Gedori.
8 Baadhi ya Wagadi walijiunga na Daudi katika ngome iliyo nyikani. Walikuwa
wanaume wapiganaji, waliofundishwa kwa mapambano, walioweza kumudu ngao
na mkuki; ambao nyuso zao zilikuwa kali kama za simba. Walikuwa wepesi kwenye
milima kama swala. 9 Kulikuwa na Eza kiongozi, Obadia wapili, Eliabu watatu,
10 Mishimana wanne, Yeremia watano, 11 Atai wasita, Elieli wasaba, 12 Yohana
wanane, Elizabadi watisa, 13 Yeremia wakumi, Makibanai wakumi na moja. 14 Wana
wa Gadi walikuwa viongozi wa jeshi. Wamwisho aliongoza mia moja, na mkubwa
aliongoza elfu moja. 15 Walikatisha Yordani kwa mwezi wa kwanza, wakati vijito
vyake vilipofurika, na kuwafukuza wote wanaoishi katika mabonde, pande zote za
mashariki na magharibi. 16 Baadhi ya wanaume wa Benjamini na Yuda walikuja
kwenye ngome kwa Daudi. 17 Daudi alienda nje kuwasalimu na kuwahutubia: "kama
mmekuja kwa amani kunisaidia, mnaweza kujiunga nami. Lakini kama mmekuja
kunisaliti kwa maadui zangu, Ee Mungu wa mababu zetu awaone na kuwakemea,
tangu sijafanya kosa." 18 Kisha roho ikaja juu ya Amasai, ambaye alikuwa kiongozi
wa wale thelathini. Amasai alisema, "Sisi ni wako, Daudi. Sisi tupo upande wako,
mwana wa Yesse. na amani iwe juu ya yeyote atakaye kusaidia. Kuwa Mungu
wako anakusaidia." Kisha Daudi akawapokea na kuwafanya wakuu wa watu wake.
19 Baadhi kutoka kwa Manase pia wakamwendea Daudi alipokuja na Wafilisti dhidi
ya Sauli katika pambano. Lakini hawakuwasaidia Wafilisti kwasababu mabwana wa
Wafilisti walishauriana na wakamfukuza Daudi. Walisema, "Atamwendea Bwana
wake Sauli na kuhatarisha maisha yetu." 20 Alipokwenda kwa Zikilagi, wanaume wa
Manase walioungana nae walikuwa Adina, Yozabadi, Yediaeli, Yozabadi, Elihu, na
Zilethai, viongozi wa maelfu wa Manase. 21 Walimsaidia Daudi kupigana na kikundi
cha wezi, maana walikuwa wanaume wa mapambano. Baadae walikuwa wakuu
katika jeshi. 22 Siku hadi siku, wanaume walikuja kwa Daudi kumsaidia, mpaka
wakawa jeshi kubwa, kama jeshi la Mungu. 23 Hii ni kumbukumbu ya wanajeshi wa
vita, walio kuja kwa Daudi Hebroni, kuupindua ufalme wa Sauli kwake, ilikutimiza
neno la Yahweh. 24 Kutoka Yuda walio beba ngao na mkuki ni 6, 800, tayari kwa vita.

25 Kutoka kwa Wasimeoni walikuwa 7, 100 wanaume wa mapambano. 26 Kutoka kwa
Walawi kulikuwa na wanaume wa mapambano 4, 600. 27 Yehoiada alikuwa kiongozi
wa uzao wa Aruni, na kwa yeye walikuwa 3, 700. 28 Kwa Zadoki, kijana, mwenye
nguvu, na mjasiri, walikuwa viongozi ishirini na mbili kwa familia ya baba yake.
29 Kutoka kwa Benjamini, kabila la Sauli, walikuwa elfu tatu. Wengi wao walibaki
waaminifu kwa Sauli mpaka muda huu. 30 Kutoka kwa Waefraimu palikuwa na
wanume wa mapambano 20, 800, wanaume maharufu kwenye familia za baba zao.
31 Kutoka kabila nusu la Manase palikuwa na wanaume elfu kumi na nane maharufu
walio kuja kufanya Daudi mfalme. 32 Kutoka kwa Isakari, palikuwa na viongozi
mia mbili walio kuwa na ufahamu wa nyakati na walijua nini Israeli ya paswa
kufanya. Ndugu zao wote walikuwa chini ya amri yao. 33 Kutoka Zebuloni palikuwa
na wanaume elfu hamsini wa mapambano, tayari kwa vita, na silaha zote za vita,
na tayari kutoa uwaminifu usio pungua. 34 Kutoka kwa Naftali palikuwa na askari
elfu moja, na pamoja nao wanaume elfu thelathini na saba wenye ngao na mikuki.
35 Kutoka kwa Wadani palikuwa na wanaume 28, 600 wameandaliwa kwa ajili ya
pambano. 36 Kutoka kwa Asheri palikuwa na wanaume elfu arobaini wameandaliwa
kwa pambano. 37 Kutoka upande wa pili wa Yordani, kutoka kwa Warubeni, Wagadi,
na nusu kabila la Manase, palikuwa na wanaume 120, 000 wameandaliwa na silaha
za kila namna kwa ajili ya pambano. 38 Wanajeshi hawa wote, waliandaliwa kwa
pambano, kuja Hebroni kwa dhumuni maalumu la kumfanya Daudi mfalme wa
Israeli yote. Israeli yote ilikubaliana na kumfanya Daudi mfalme. 39 Walikuwa na
Daudi siku tatu, kula na kunywa, kwa kuwa ndugu zao waliwapa mahitaji ya kwenda
nayo. 40 Kwa kuongezea, wao walio kuwa karibu nao, kwa umbali wa Isakari na
Zebuloni na Naftali, walileta mkate kwa punda, ngamia, ng'ombe, na keki, mvinyo,
mafuta, ng'ombe, na kondoo, kwa kuwa Israeli walikuwa wana sherehekea

# 13

1 Daudi akashuriana na wakuu wa jeshi la maelfu na mamia, na kila kiongozi.
2 Daudi akasema kwa kusanyiko la Isaraeli, “Kama itakuwa vyema, na kama hii
inatoka kwa Yahweh Mungu wetu, na tutume wajumbe kila sehemu kwa ndugu
zetu walio baki maeneo yote ya Israeli, na kwa makuhani na Walawi walio kwenye
miji yao. Waambiwe wajiunge nasi. 3 Na tulete sanduku la Mungu wetu, kwa
kuwa hatukutafuta mapenzi yake katika siku za Sauli.” 4 Kusanyiko lote liliafiki
kufanya haya yote, kwa kuwa yalionekana sawa machoni pa watu wote. 5 Kwaiyo
Daudi akakusanya Israeli yote, kutoka mto Shihori ulio Misri hadi Lebo Hamathi,
kuleta sandaku la Mungu kutoka Kiriathi Yearimu. 6 Daudi na Israeli yote walienda
mpaka Baala, ambayo ni, Kiriathi Yearimu, ambao ni ya Yuda, kuleta sanduku
la Mungu, ambalo linaitwa kwa jina la Yahweh, Yahweh, ambaye ameketi juu ya
makerubi. 7 Kwaiyo wakaketisha sanduku la Mungu juu ya chombo kipya cha matairi.
Wakaleta nje ya nyumba ya Abinadabu. Uza na Ahio walikuwa wakilinda hicho
chombo. 8 Daudi na Israeli yote walikuwa wakishangilia mbele za Mungu kwa nguvu
zao zote. Walikuwa wakiimba na vyombo vya uzi, vinubi, upatu, na tarumbeta.
9 Walipo kuja eneo la kupeta mazao huko Kidoni, Uza alinyoosha mkono wake
kuzuia sandaku, sababu ng'ombe aliyekuwa amebeba sanduku aliyumba. 10 Hasira
ya Yahweh ikawaka juu ya Uza, na Yahweh akamua kwasababu Uza alishika na
mkono wake sanduku. Akafa pale mbele za Mungu. 11 Daudi alipatwa na hasira
kwa kuwa Yahweh alimshambulia Uza. Hiyo sehemu inaitwa Perezi Uza hadi leo.
12 Daudi alimuogopa Mungu hiyo siku. Akasema, “Nawezaje kuleta sanduku la
Mungu nyumbani mwangu?” 13 Kwaiyo Daudi hakuleta sanduku kwenye mji wa
Daudi, lakini aliweka pembeni mwa nyumba ya Obedi Edomu Mgiti. 14 Sanduku la

Mungu lilibaki nyumbani mwa Obedi Edomu kwa miezi mitatu. Kwaiyo Yahweh
akabariki nyumba yake na yote aliyo miliki.

# 14

1 Kisha Hiramu mfalme wa Tire alituma wajumbe kwa Daudi, na miti ya mierezi,
maseremala, na wajenzi. Walijenga nyumba kwa ajili yake. 2 Daudi alijua kuwa
Yahweh alimfanya kuwa mfalme juu ya Waisraeli, na hivyo ufalme wake ulitukuzwa
juu sana kwa ajili ya watu wa Israeli 3 Ndani ya Yerusalemu, Daudi aliongeza
wake, na akawa baba wa wana wengi na mabinti. 4 Haya yalikuwa majina ya
watoto waliozaliwa nae huko yerusalemu: Shammua, Shobabu, nathani, Solimoni,
5 Ibhari, Elishama, Elpeleti, 6 Noga, Nefegi, Jafia, 7 Elishama, Beliada, na Elifeleti.
8 Sasa tangu Wafilisti waliposikia Daudi amepakwa mafuta kama mfalme juu ya
Waisraeli, wote walitoka nje kwenda kumtafuta. Lakini Daudi alisikia kuhusu hilo
nae akaenda nje kinyume nao. 9 Sasa wafilisti walikuja na kufanya shambulio
katika bonde la Refaimu. 10 Kisha Daudi akaomba msaada kwa Mungu. Akasema,
“Je niwashambulie Wafilisti? Utanipa ushindi juu yao?” Yahweh akamwambia,
“ Shambulia, kwa uhakika nitawakabidhi kwako.” 11 Kwa hivyo wakaja Baali
Perazimu na akawashinda. Akasema, “ Yahweh kapasua maadui zangu kwa mkono
wangu kama vile mpasuko wa mafuriko ya maji.” Hivyo jina la sehemu ile
likawa Baali Perazimu. 12 Wafilisti walitelekeza miungu yao pale, na Daudi akatoa
amri wateketezwe kwa moto. 13 Kisha Wafilisti wakavamia kwa mara nyingine
tena. 14 Hivyo Daudi akaomba msaada kwa Mungu tena. Mungu akamwambia, “
Usiwashambulie kwa mbele, lakini wazunguke kwa nyuma yao na uwajie kupitia
misitu ya balisamu. 15 Utakaposikia sauti ya wanajeshi wanatembea kwenye upepo
uvumao kutoka juu ya miti ya balisamu, kisha shambulia kwa nguvu. Fanya hivyo
kwasababu Mungu atakutangulia kwenda kuwashambulia majeshi ya wafilisti.”
16 Hivyo Daudi alifanya kama Mungu alivyo muamuru. Aliwashinda jeshi la Wafilisti
kutoka Gibeoni mpaka Gezeri. 17 Kisha umaarufu wa Daudi ukaenda katika nchi zote,
na Yahweh akasababisha mataifa yote kumuhofia.

# 15

1 Daudi akajingea nyumba zake katika mji wa Daudi. Akaanda sehemu kwa
ajili ya sanduku la Mungu na hema lake. 2 Kisha Daudi akasema, “Walawi pekee
ndio watabeba sanduku la Mungu, kwa kuwa walichaguliwa na Yahweh kubeba
sanduku la Yahweh, na kumtumikia milele.” 3 Kisha Daudi akakusanya Israeli yote
Yerusalemu, kuleta sanduku la Yahweh sehemu aliyo iandaa. 4 Daudi akakusanya
uzao wa Aruni na Walawi pamoja. 5 Kutoka uzao wa Kohathi, palikuwa na Urieli
kiongozi na ndugu zake, wanaume 120. 6 Kutoka uzao wa Merari, palikuwa na Asaia
kiongozi na ndugu zake, wanaume 220. 7 Kutoka uzao wa Gerishomu, palikuwa na
Yoeli kiongozi na ndugu zake, wanaume 130. 8 Kutoka uzao wa Elizafani, palikuwa na
Shemaia kiongozi na ndugu zake, wanaume 200. 9 Kutoka uzao wa Hebroni, palikuwa
na Elieli kiongozi na ndugu zake, wanaume themanini. 10 Kutoka uzao wa Uzieli,
palikuwa na Aminadabu kiongozi na ndugu zake, wanaume 112. 11 Daudi akaagiza
Zadoki kuitwa na Abiathari kuhuani, na Walawi Urieli, Asaia, Yoeli, Shemaia, Elieli,
na Aminadabu. 12 Akasema, “Nyinyi ni viongozi wa familia za Kilawi. Jiwekeni
wakfu, nyie na ndugu zenu, ilikwamba mlete sanduku la Yahweh, Mungu wa Israeli,
kwenye sehemu niliyo iandaa. 13 Mara ya kwanza hamkubeba. Ndio maana Yahweh
Mungu wetu akawa na hasira kwetu, kwa kuwa hatuku mtafuta wala kutii amri
yake.” 14 Hivyo makuhani na Walawi waka jiweka wakfu iliwaweze kuleta sanduku
la Yahweh, Mungu wa Israeli. 15 Walawi wakabeba sanduku la Mungu katika mabega

yao na nguzo, kama Musa alivyo amuru-kwa kufuata sheria zilizo tolewa na Yahweh.
[16] Daudi akazungumza na viongozi wa Walawi kuwapangia ndugu zao kuwa wana
muziki wenye vyombo vya muziki, vyombo vya uzi, vinubi na upatu, kwa kupiga
kwa sauti na furaha wakipaza sauti zao. [17] Hivyo Walawi wakamchagua Hemani
mwana wa Yoeli na mmoja wa kaka zake, Asafu mwana wa Berekia. Pia walimchagua
ndugu wa uzao wa Merari na Ethani mwana wa Kushaia. [18] Pamoja nao walikuwa
ndugu wa daraja la pili: Zekarai, Yaazieli, Shemiramothi, Yehieli, Uni, Eliabu, Benaia,
Maasaeia, Matithia, Elifelehu, Mikineaia, Obedi Edomu, na Yeieli, mlinzi wa lango.
[19] Wanamuziki Hemani, Asafu, na Ethani walichaguliwa kupiga upatu wa shaba.
[20] Zekaria, Azieli, Shemiramothi, Yehieli, Uni Eliabu, Maaseia, na Benaia walicheza
vyombo vya uzi. [21] Matithia, Elifelehu, Mikineia, Obedi Edomu, Yeieli, na Azazia
waliongoza njia na vinubi. [22] Kenania, kiongozi wa Walawi, aliongoza uimbaji
sababu alikuwa mwalimu wa muziki. [23] Berekia na Elikana walikuwa walinzi wa
sanduku. [24] Shebania, Yoshafati, Nethanieli, Amasai, Zekaria, Benaia, na Eliezeri,
makuhani, walikuwa wa kupuliza matarumbeta mbele ya sanduku la Mungu. Obedi
Edomu na Yehia walikuwa walinzi wa sanduku. [25] Hivyo Daudi, wazee wa Israeli, na
wakuu wa maelfu wakaenda kuchukua sanduku la agano la Yahweh kutoka nyumba
ya Obedi Edomu kwa shangwe. [26] Wakati Mungu alipo wasaidia Walawi kubeba
sanduku la agano la Yahweh, walitoa ng'ombe saba na mbuzi [27] Daudi alivishwa
joho safi la maridadi, pamoja na Walawi walio beba sanduku, waimbaji, na Kenania,
kiongozi wa nyimbo na waimbaji. Daudi alivaa juu ya joho lake naivera. [28] Hivyo
Israeli yote wakaleta sanduku la agano la Yahweh na kelele za shangwe, na sauti
za tarumbeta, ngoma za saani, na vyombo vya uzi na vinubi. [29] Lakini sanduku la
Yahweh lilivyokuja kwa mji wa Daudi, Mikali binti wa Sauli, alitazama nje ya dirisha,
Akamuona Mfalme Daudi akicheza na kusherehekea. Kisha akamdharau moyoni
mwake.

# 16

[1] Wakaleta ndani Sanduku la Mungu na kuweka katika ya hema ambalo Daudi
aliandaa. Kisha wakatoa sadaka ya kuteketeza na sadaka ya ushirika mbele ya
Mungu. [2] Daudi alipo maliza kutoa dhabiu ya kuteketeza na sadaka za ushirika,
aliwabariki watu kwa jina la Yahweh. [3] Alisambaza kwa kila Misraeli, mwanaume
na mwanamke, kipande cha mkate, na kipande cha nyama, na keki ya mzabibu.
[4] Daudi aliewapangia baadhi ya Walawi kutumika mbele ya sanduku la Yahweh, na
kusheherekea, kushukuru na kumsifu Yahweh, Mungu wa Israeli. [5] Hawa Walawi
walikuwa Asafu kiongozi, wa pili kutoka kwake Zekaria, Yeieli, Shemiramothi, Yehieli,
Matithia, Eliabu, Benaia, Obedi Edomu, na Yeieli. Hawa walikuwa wacheze na
vyombo vya uzi na vinubi. Asafu alikuwa apige upatu, kwa kelele. [6] Benaia na
Yahazieli walikuwa wakupiga tarumbeta kila mara, mbele sanduku la agano la
Mungu. [7] Kisha katika hiyo siku Daudi akawachagua Asafu na kaka zake kuimba
hii nyimbo ya shukurani kwa Yahweh. [8] Mpeni shukurani Yahweh, liitieni jina
lake; fahamisheni mataifa matendo yake. [9] Mwiimbieni, imbeni sifa kwake; semeni
matendo yake ya ajabu. [10] Jisifuni katika jina lake takatifu; mioyo ya wanao mtafuta
Yahweh ishangilie. [11] Mtafute Yahweh na nguvu zake; tafuteni uwepo wake siku
zote. [12] Kumbukeni matendo aliyo ya fanya kwenu, miujiza yake na amri za kinywa
chake, [13] enyi uzao wa Israeli mtumishi wake, enyi watu wa Yakobo, wateule wake.
[14] Yeye ni Yahweh, Mungu wetu. Amri zake zipo duniani kote. [15] Tunzeni agano lake
akilini mwenu milele, neno alilo liamuru kwa vizazi elfu moja. [16] Anakumbuka agano
alilo lifanya na Ibrahimu, na nadhiri yake kwake Isaka. [17] Hili ndilo alilo lithibitisha
kwa Yakobo kama amri maalumu, na kwa Israeli kama agano la milele. [18] Alisema,

“Nitakupa nchi ya Kanani kama sehemu ya urithi wako.” [19] Nilisema hili mlipo kuwa
wachache kwa idadi, wachache sana, mlipo kuwa wageni katika nchi. [20] Walienda
taifa hadi taifa, kutoka ufalme mmoja hadi mwingine. [21] Hakuwaruhusu yeyote
awatese; aliwahadhibu wafalme kwa ajili yao. [22] Alisema, “ Msiwaguse wapakwa
mafuta wangu, na msiwadhuru manabii wangu.” [23] Imbeni kwa Yahweh, dunia yote;
tangazeni wokovu wake siku hadi siku. [24] Kirini utukufu wake kwa mataifa, matendo
yake makuu kwa mataifa yote. [25] Kwa kuwa Yahweh ni mkuu na ni wakusifiwa
sana, na ni wakuogopewa kuliko miungu yote. [26] Kwa kuwa miungu ya mataifa ni
sanamu, lakini ni Yahweh aliye umba mbingu. [27] Uzuri wa ajabu na utukufu upo
uweponi mwake. Uwezo na furaha upo kwake. [28] Mpeni sifa Yahweh, enyi koo
za watu, mpeni sifa Yahweh utukufu na uwezo; [29] Mpeni Yahweh utukufu upasao
jina lake. Leta sadaka na mje kwake. Muinamieni Yahweh katika utakatifu wa uzuri
wake. [30] Mtetemeke mbele zake, dunia yote. Dunia imeimarishwa; haiwezi kutikisika.
[31] Mbingu nazo ziwe nafuraha, na dunia ifurahi; na wasema kwa mataifa yote,
“Yahweh anatawala.” [32] Bahari na ingurume, na inayo ijaza ipige kelele kwa furaha.
Mashamba yawe na furaha tele, na vyote vilivyomo ndani yake. [33] Na miti iliyopo
misituni ipige kelele kwa Yahweh, kwa kuwa anakuja kuhukumu dunia. [34] Toeni
shukurani kwa Yahweh, kwa kuwa ni mwema, uaminifu wa agano lake la dumu
ata milele. [35] Kisha sema, “Tuokoe, Mungu wa wokovu wetu. Tukusanye pamoja
na utuokoe kutoka kwa mataifa mengine, ilikwamba tutoe shukurani kwa jina lako
takatifu na tufurahi katika sifa zako.” [36] Na Yahweh, Mungu wa Israeli, asifiwe kutoka
milele na milele. Watu wote wakasema, “Amina” na wakamsifu Yahweh. [37] Hivyo
Daudi akamwacha Asafu na kaka zake pale mbele ya sanduku la Yahweh, kutumika
daima mbele ya sanduku, kama kazi za kila siku zilivyo itaji. Obedi Edomu pamoja
na ndugu sitini na nane walijumuishwa. [38] Obedi Edomu mwana wa Yeduthuni,
pamoja na Hosa, walikuwa wawe walinzi wa lango. [39] Zadoki kuhani na makuhani
wenzake walikuwa watumike mbele ya hema la Yahweh katika mahali pa juu huko
Gibeoni. [40] Walikuwa watoe sadaka za kuteketeza kwa Yahweh kwenye madhabahu
ya sadaka za kuteketeza daima asubui na jioni, kwa mujibu wa yote yalio andikwa
katika amri za Yahweh, aliyo wapa Waisraeli kama sheria. [41] Hemani na Yeduthuni
walikuwa nao, pamoja na walio chaguliwa kwa jina, kumpa shukurani Yahweh,
kwasababu uaminifu wa agano lake la dumu ata milele [42] Hemani na Yeduthuni
walikuwa viongozi wa wao waliopiga tarumbeta, upatu, na vyombo vingine kwa
muziki wa kumuabudu Mungu. Wana wa Yeduthuni walilinda lango. [43] Kisha watu
wote walirudi nyumbani, na Daudi akarudi kubariki nyumba yake.

# 17

[1] Ikawa baada ya mfalme kuwa katika nyumba yake, akasema kwa Nathani yule
nabii, “Angalia, nina ishi katika nyumba iliyo jengwa na mierezi, lakini sanduku
la agano la Yahweh lipo kwenye chini ya hema.” [2] Kisha Nathani akasema kwa
Daudi, Nenda, fanya yalio moyoni mwako, kwa kuwa Mungu yupo nawe.” [3] Lakini
usiku huo neno la Mungu lilimjia Nathani, nakusema, [4] “Nenda umwambie Daudi
mtumishi wangu, 'Hivi ndivyo Yahweh asemavyo: Hautanijengea nyumba ya kuishi.
[5] Kwa kuwa sijaishi katika nyumba toka ile siku niliyo ileta Israeli hadi leo. Badala
yake, nimeishi ndani ya hema, hema la kukusanyikia, sehemu mbali mbali. [6] Katika
sehemu zote nilizo enda na Israeli, niliwai kusema lolote kwa viongozi wa Israeli
niliyo wachagua kuwa chunga watu wangu, kwa kusema, “Kwa nini haujanijengea
mimi nyumba ya mierezi?”” [7] “Kisha sasa, mwambie mtumishi wangu Daudi, 'Hili
ndilo Yahweh wa majeshi anasema: Nilikuchugua kutoka malishoni, kufuata kondoo,
ilikwamba uwe mtawala wa watu wangu Waisraeli. [8] Nimekuwa nawe pote ulipo

enda na nimewakata maadui zako wote, na na nitakufanyia jina, kama jina la
wakuu wa dunia. 9 Nitachagua sehemu ya watu wangu Israeli na nitawapanda
hapo, iliwaishi sehemu yao na wasisumbuke tena. Watu wa ovu hawata watesa tena,
kama walivyo fanya mwanzo, 10 kama walivyo kuwa wakifanya toka siku zile nilipo
waamuru waamuzi kuwa juu ya watu wangu Waisraeli. Kisha nitawatiisha maadui
zako wote. Zaidi sana nina kwambia kwamba mimi, Yahweh, nitakujengea nyumba.
11 Itakuja kuwa hapo siku zako zitapo timia za wewe kwenda kwa baba zako,
nitainua uzao wako baada yako, na mmoja wa uzao wako nitaimarisha ufalme wake.
12 Yeye atanijengea nyumba, na nitaimarisha kiti chake cha enzi milele. 13 Nitakuwa
baba kwake, naye atakuwa mwana wangu. Sitaondoa uwaminifu wa Agano langu
kwake, kama nilivyo ondoa kwa Sauli, aliye tawala kabla yako. 14 Nitamweka juu ya
nyumba yangu na katika ufalme wangu milele, na kiti chake cha enzi kitaimarishwa
milele." 15 Nathani akanena haya kwa Daudi na kumtaarifu, na akamwambia kuhusu
maono yote. 16 Kisha Daudi mfalme akaenda ndani na kuketi mbele za Yahweh;
akasema, "Mimi ni nani, Yahweh Mungu, na familia yangu ni nini, hadi unilete
umbali huu? 17 Hili lilikuwa jambo dogo machoni pako, Mungu. Umezungumzia
familia ya mtumishi wako kwa muda mrefu ujao, na umenionyesha vizazi vijavyo,
Yahweh Mungu. 18 Nini zaidi mimi, Daudi, niseme? Umemheshimu mtumishi
wako. Umemtambua kwa kipekee mtumishi wako. 19 Yahweh, kwa ajili ya mtumishi
wako, na kutimiza kusudi lako, umefanya hili ilikudhihirisha matendo yako makuu.
20 Yahweh, hakuna aliye kama wewe, na hakuna Mungu zaidi yako, kama tulivyo sikia
mara zote. 21 Ni taifa gani duniani kama watu wako Israeli, ambaye wewe, Mungu,
uliwaokoa kutoka Misri iliwawe watu wako, kujifanyia jina lako kwa matendo makuu
na yahajabu? Uliondoa mataifa mbele za watu wako, uliye waokoa kutoka Misri.
22 Ulifanya Israeli watu wako milele, na wewe, Yahweh, ukawa Mungu wao. 23 Hivyo
sasa, Yahweh, ile ahadi uliyo iweka kuhusu mtumishi wako na nyumba yake itimizwe
milele. Fanya kama ulivyo nena. 24 Jina lako na litukuzwe milele na kuwa kuu, ili
watu waseme, 'Yahweh wa majeshi ni Mungu wa Israeli,' na nyumba yangu, mimi
Daudi, mtumishi wako ikiwa imeimarishwa mbele zako. 25 Kwa kuwa wewe, Mungu
wangu, umedhihirisha kwa mtumishi wako utamjengea nyumba. Hiyo ndio sababu,
mimi mtumishi wako, nimepata ujasiri wa kuomba kwako. 26 Sasa, Yahweh, wewe
ni Mungu, na umefanya hii ahadi nzuri kwa mtumishi wako: 27 Sasa imekupendeza
kubariki nyumba ya mtumishi wako, iliiendelee milele mbele zako. Wewe, Yahweh,
umeibariki, na itabarikiwa milele."

# 18

1 Baada ya haya Daudi akawashambulia Wafilisti na kuwashinda. Alichukuwa
Gathi na vijiji vyake katika utawala wa Wafilisti. 2 Kisha akamshinda Moabu, na
Wamoabu wakawa watumishi wa Daudi na wakamlipa ushuru maalumu. 3 Daudi
kisha akamshinda Hadadezeri, mfalme wa Zoba huko Hamathi, wakati Hadadezeri
alipo kuwa akisafiri kuimarisha utawala wake kwa Mto wa Frati. 4 Daudi akateka
magari ya farasi elfu, wanaume wa farasi elfu saba, na wanajeshi wa miguu elfu
ishirini. Daudi aliwajeruhi farasi wote wagari, lakini akahifadhi baadhi kwa ajili
ya magari ya farasi mia moja. 5 Waaramia wa Damasko walipo kuja kumsaidia
Hadadezeri mfalme wa Zoba, Daudi aliua wanaume elfu ishirini na mbili wa
Kiaramia. 6 Kisha Daudi akaweka vikosi huko Aramu ya Damasko, na Waaramia
wakawa watumishi wake na wakamletea ushuru maalaumu. Yahweh alimpatia
Daudi ushindi popote alipoenda. 7 Daudi alichukua ngao za dhahabu zilizo kuwa
kwa watumishi wa Hadadezeri na kuleta Yerusalemu. 8 Kutoka Tibhathi na Kuni,
miji ya Hadadezeri, Daudi alichukuwa shaba nyingi sana. Ilikuwa shaba hii ambayo

baadae Sulemani alifanya saani ya shaba, nguzo, na vifaa vya shaba. 9 Wakati
Toi, mfalme wa Hamathi, alipo sikia kuwa Daudi ameshinda majeshi yote ya
Hadadezeri mfalme wa Zoba, 10 Toi akamtuma Hadoramu mwanae kwa Mfalme
Daudi kumsalimia na kumbariki, kwasababu Daudi amepigana na Hadadezeri na
kumshinda, na kwasababu Hadadezeri alifanya vita na Toi. Hadoramu alipeleka
vifaa vya fedha, dhahabu, na shaba. 11 Mfalme Daudi alivitenga hivi vitu kwa ajili
ya Yahweh, pamoja na fedha na dhahabu aliyo ibeba kutoka kwa mataifa yote:
Edomu, Moabu, watu wa Amoni, Wafilisti, na Waamaleki. 12 Abishai mwana wa
Zeruia akawaua Waedomi elfu kumi na nane katika Bonde la Chumvi. 13 Alieka
vikosi huko Edomu, na Waedomi wote wakawa watumishi wa Daudi. Yahweh alimpa
Daudi ushindi pote alipoenda. 14 Daudi alitawala Israeli yote, na alitenda haki na
utaua kwa watu wote. 15 Yoabu mwana wa Zeruia walikuwa mkuu wa jeshi, na
Yehoshafati mwana wa Ahiludi alikuwa mtunza kumbukumbu. 16 Zadoki mwana wa
Ahitubi na Ahimeleki mwana wa Abiathari walikuwa makuhani, na Shavisha alikuwa
mwandishi. 17 Benaia mwana wa Yehoiada alikuwa mwangalizi wa Wakerethi na
Wapelethi, na wana wa Daudi walikuwa washauri wakuu wa mfalme.

# 19

1 Ikajakuwa baadae kwamba Nahashi, mfalme wa watu wa Amoni, akafa, na
mwanae akawa mfalme baada yake. 2 Daudi akasema, “Nitaonyesha ukarimu kwa
mwana wa Hanuni wa Nahashi, kwasababu baba yake alionyesha ukarimu kwangu.”
Hivyo Daudi akatuma wajumbe kumfariji kuhusu baba yake. Watumishi wa Daudi
wakaingia nchi ya Waamoni na kumfuata Hanuni, ilikumfariji. 3 Lakini viongozi
wakamwambia Hanuni, “Unadhani Daudi anamheshimu baba yako sababu ametuma
watu kukufaraji? Je watumishi wake hawajaja kutadhimini nchi iliwaipindue?
4 Hanuni akawakamata watumishi wa Daudi, akawanyoa, akakata mavazi ya nusu
kwenye kiuno kushuka, na kuwarudisha. 5 Walipo eleza haya kwa Daudi, alienda
kukutana nao, kwa kuwa walifedheeka sana. Mfalme akasema, “Bakini Yeriko hadi
ndevu zenu ziote tena, kisha mrudi.” 6 Waamoni walipoona wamekuwa kikwazo
kwa Daudi, Hanuni na Waamoni walituma talanta elfu moja za fedha kukodisha
magari ya farasi kwa Waaremei na wanaume wa farasi kutoka Naharaimu, Maka, na
Zoba. 7 Waliwakodishia magari ya farasi elfu thelathini na mbili pamoja na mfalme
wa Maka na watu wake, walio kuja na kueka kambi mbele ya Medeba. Waamoni
walijikusanya pamoja kutoka miji yao, na wakaja kwa vita. 8 Daudi alipo sikia,
alimtuma Yoabu na wanajeshi wake wote. 9 Watu wa Amoni walikuja na kupanga
mstari kwa ajili ya pambano katika lango la mji, wafalme waliokuja walikuwa
peke yao katika shamba. 10 Yoabu alipoona mistari ya pambano imemzunguka
mbele na nyuma, alichagua wapambanaji shupavu wa Israeli na kuwa panga dhidi
ya Waaremi. 11 Wanajeshi wengine wote, aliwaeka chini ya Abishai kaka yake,
akawapanga kwa mstari dhidi ya Amoni. 12 Yoabu akasema, “Kama Waaremi
wananguvu kunizidi, kisha wewe, Abishai, lazima uniokoe. Lakini kama jeshi la
Waamoni lina nguvu kukuzidi, nitakuja kukuokoa. 13 Kuwa thabiti, natujionyeshe
kwa watu wetu kuwa ni wenye nguvu na kwa miji ya Mungu wetu, kwa kuwa
Yahweh ata fanya lililo jema kwa kusudi lake.” 14 Hivyo Yoabu na wanajeshi wasogea
kwenye pambano dhidi ya Waaremi, walio lazimika kukimbia mbele ya jeshi la
Waisraeli. 15 Jeshi la Waamoni walipoona kuwa Waaremi wamekimbia, wao pia
wakamkimbia kaka yake Yoabu Abishai na kurudi mjini. Kisha Yoabu akarudi
kutoka kwa watu wa Amoni na kurudi Yerusalemu. 16 Waaremi walipoona kuwa
wanashindwa na Waisraeli, wakatuma msaada nyuma ya Mto Frati, na Shofaki mkuu
wajeshi la Hadadezeri. 17 Daudi alipo ambiwa haya, akakusanya Israeli yote, akuvuka
Yordani, na kuja juu yao. Alipanga jeshi kwa ajili ya pambano dhidi ya Waaremi, na

wakapigana nao. 18 Waaremi waliwakimbia Waisraeli, na Daudi akaua waendesha
magari ya farasi ya Waaremi elfu saba na wanajeshi wa miguu elfu arobaini. Pia
alimuua Shopaki, mkuu wa jeshi. 19 Wafalme wote walio kuwa watumishi wa
Hadadezeri walipoona kuwa wameshindwa na Israeli, walifanya amani na Daudi
na kumtumikia. Hivyo watu wa Aramu hawakuwa tayari kuwasaidia Waamoni.

# 20

1 Ikaja kuwa wakati wa mvua, kipindi wafalme uenda vitani, Yoabu akaongaza jeshi
kwenda kupambana na kusikitisha nchi ya Waamoni. Aliienda na kuteka Raba. Daudi
alibaki Yerusalemu. Yoabu alishambulia Raba na kuishinda. 2 Daudi alichukuwa
taji la mfalme wao kichwani mwake, na akagundua linauzito wa talanta moja ya
dhahabu, na ndani yake kulikuwa na mawe ya thamani. Taji liliwekwa kichwani
mwa Daudi, na akaleta mali nyingi za mji. 3 Aliwaleta watu walio kuwa ndani ya mji
na kuwalazimisha wafanye kazi kwa msumeno na jembe na shoka. Daudi aliwataka
watu wote wa mji kufanya kazi hii. Daudi na jeshi lote wakarudi Yerusalemu.
4 Ilikuwa baada ya haya kukawa na pambano huko Gezeri na Wafilisti. Sibekai
Mhushathi akamua Sipai, mmoja wa uzao wa Refaimu, na wa Filisti wakazidiwa.
5 Ikawa tena katika pambano na Wafilisti huko Gobu, kwamba Elhanani mwana
wa Yari Mbethilehemu akamua Lami kaka wa Goliathi Mgiti, ambaye mkuki wake
ulikuwa kama gongo la mshonaji. 6 Ikaja kuwa tena katika pambano lingine huko
Gathi kwamba mwanaume mmoja aliye mrefu sana mwenye vidole sita kila mkono
na vidole sita mguuni. Naye alikuwa pia wa uzao wa Refaimu. 7 Alipo dhihaki jeshi la
Israeli, Yehonadabu mwana wa Shimea, kaka wa Daudi, akamuua. 8 Hawa walikuwa
uzao wa Refaimu wa Gathi, na waliuawa na mkono wa Daudi na mkono wa wanajeshi
wake.

# 21

1 Adui akainuka dhidi ya Israeli na kumchochea Daudi kuhesabu Israeli. 2 Daudi
akamwabia Yoabu na kwa wakuu wa Jeshi, “Nenda, wahesabu watu wa Israeli kutoka
Beerisheba mpaka Dani na uniletee taarifa, ilinijue idadi yao.” 3 Yoabu akasema,
“Yahweh na afanya jeshi lake mara mia zaidi ya lilivyo. Lakini bwana wangu mfalme,
kwani wote hawamtumikii bwana wangu? kwa nini bwana wangu anataka hili? Kwa
nini ulete hatia kwa Israeli?” 4 Lakini neno la mfalme halikubadilika kwa Yoabu.
Hivyo Yoabu akaondoka na kwenda Israeli yote. Kisha akarudi Yerusalemu. 5 Yoabu
akatoa taarifa ya idadi ya jumla ya wanaume wa mapambano kwa Daudi. Kulikuwa
ndani ya Israeli wanaume 1, 100, 000 walio beba upanga. Yuda peke yake kulikuwa
na wanajeshi 470, 000. 6 Lakini Levi na Benjamini hawaku hesabiwa miongoni mwao,
kwa kuwa amri ya mfalme ilimuudhi Yoabu. 7 Mungu alikwazika na hili tendo,
akashambulia Israeli. 8 Daudi akamwambia Mungu, “Nimetenda dhambi kubwa kwa
kufanya hili. Sasa chukua hatia ya mtumishi wako, nimetenda kwa ujinga sana.”
9 Yahweh akamwambia Gadi, nabii wa Daudi, 10 “Nenda useme kwa Daudi, “Hili ndilo
Yahweh anasema: Ninakupa maamuzi matatu. Chagua moja wapo.” 11 Hivyo Gadi
akaenda kwa Daudi na kusema, “Yahweh anasema hivi, 'Chagua moja ya haya: 12 kati
ya miaka mitatu ya ukame, miezi mitatu unakimbizwa na adui zako na kupatwa na
upanga wao, au siku tatu za upanga wa Yahweh, yani, pigo katika nchi, malaika wa
Yahweh akiharibu nchi yote ya Israeli.' Hivyo sasa, amua jibu gani ni mpelekee yeye
aliye nituma.” 13 Kisha Daudi akamwambia Gadi, “Nipo katika shida kubwa sana.
Acha nianguke katika mikono ya Yahweh kuliko kuangukia mikono ya mwanadamu,
sababu matendo yake ya rehema ni makubwa mno.” 14 Hivyo Yahweh akatuma
pigo Israeli, na watu elfu sabini wakafa. 15 Mungu akatuma malaika Yerusalemu
kuiharibu. Wakati alipo taka kuiharibu, Yahweh akatazama na kubadili nia yake

kuhusu shambulio. Akasema kwa malaika wa uharibifu, “Imetosha! Rudisha mkono
wako.” Wakati huo malaika wa Yahweh alikua amesimama eneo la kupeta la Orinani
Myebusi. 16 Daudi akatazama juu na kuona malaika wa Yahweh amesimama kati ya
nchi na mbingu, akiwa na upanga mkonono mwake akiuelekeza Yerusalemu. Kisha
Daudi na wazee, wakiwa wamevaa magunia, wakalala chini uso ukiwa kwenye ardhi.
17 Daudi akamwambia Mungu, “Sio mimi niliye amuru jeshi kuhesabiwa? Nimefanya
hichi kitu kiovu. Lakini hawa kondoo, wamefanya nini? Yahweh Mungu wangu!
Acha mkono wako unipige mimi na familia yangu, lakini usiache pigo iliendelee
kubaki kwa watu wako.” 18 Hivyo malaika wa Yahweh akamuamuru Gadi kusema
kwa Daudi, kwamba Daudi aende juu na kujenga madhabahu ya Yahweh katika
eneo la kupeta la Oranani Myebusi. 19 Daudi akaenda kama Gadi alivyo muelekeza
cha kufanya kwa jina la Yahweh. 20 Wakati Orinani akipepeta ngano, aligeuka na
kumuona malaika. Yeye na wana wake wanne wakajificha. 21 Wakati Daudi alipo
kuja kwa Orinani, Orinani akatazama na kumuona Daudi. Aliacha eneo la kupeta
na akamuinamia Daudi uso wake ukiwa kwenye ardhi. 22 Kisha Daudi akasema
kwa Orinani, “Niuzie hili eneo la kupeta, iliniweze kumjenga Yahweh madhabahu.
Nitalipa gharama yote, ili pigo liondolewe kwa watu.” 23 Orinani wakwambia Daudi,
“Chukuwa kama lako, bwana wangu mfalme. Fanya nalo linalo kupendeza. Tazama,
nitakupa ng'ombe kwa sadaka ya kuteketeza, vifaa vya kupeta kwa ajili ya mbao, na
ngano kwa sadaka ya mbegu; nitakupa yote wewe.” 24 Mfalme Daudi akamwambia
Orinani, “Hapana, nina sisitiza kununua kwa bei yote. Sitachukua kilicho chako
na kutoa kama sadaka ya kuteketeza kwa Yahweh kama haitanighramu chochote.”
25 Hivyo Daudi akalipa shekeli mia sita ya dhahabu kwa hilo eneo. 26 Daudi akajenga
madhabahu ya Yahweh pale na kutoa sadaka za kuteketezwa na sadaka za ushirika.
Akamuita Yahweh, aliye mjibu kwa moto kutoka mbinguni kwenye madhabahu
ya sadaka za kuteketezwa. 27 Kisha Yahweh akampa agizo malaika, na malaika
akarudisha upanga kwenye mfuko wake. 28 Daudi alipo ona kuwa Yahweh amemjibu
kwenye eneo la kupeta la Orinani Myebusi, alitoa dhabihu pale pale kwa wakati huo.
29 Sasa kwa wakati huo, hema la kuabudia la Yahweh, ambalo Musa alilitengeneza
nyikani, na madhabahu ya sadaka za kuteketezwa, zilikuwa sehemu ya juu huko
Gibeoni. 30 Walakini, Daudi hakuweza kwenda huko kumuliza Mungu muelekeo,
kwa kuwa alikuwa anaogopa upanga wa malaika wa Yahweh.

# 22

1 Kisha Daudi akasema, “Hapo ndipo nyumba ya Yahweh Mungu itakuwepo,
na madhabahu ya sadaka za kuteketezwa za Israeli.” 2 Hivyo Daudi akaagiza
watumishi wake wawakusanye pamoja wageni wote wanao ishi katika nchi ya Israeli.
Aliwapangia kuwa wachonga mawe, kuchonga matofali ya mawe, ilikuweza kujenga
nyumba ya Mungu. 3 Daudi alisambaza idadi kubwa ya chuma kwa ajili ya misumari
na vitasa vya kuweka kwenye malango. Pia alitoa shaba zaidi kushinda kipimo, 4 na
miti ya mierezi zaidi ya kipimo. (Wasidoni na Watiria walileta mboa nyingi za mierezi
kwa Daudi azihesabu.) 5 Daudi akasema, “Mwanangu Sulemani ni mdogo na hana
uzoefu, na nyumba itayo jengwa kwa Yahweh lazima iwe maridadi, ilikwamba iwe
maarufu na ya utukufu kwa nchi zingine. Hivyo nitaanda ujenzi wake.” Hivyo Daudi
akafanya maandalizi ya kina kabla ya mauti yake. 6 Akaagiza Sulemani mwanae
kuitwa na kumuamuru ajenge nyumba ya Yahweh, Mungu wa Israeli. 7 Daudi
akasema kwa Sulemani, “Mwanangu, ilikuwa dhamira yangu kujenga nyumba
mwenyewe, kwa ajili ya jina la Yahweh Mungu wangu. 8 Lakini Yahweh alikuja
kwangu na kusema, 'Wewe umemwaga damu nyingi na umepigana mapambono
mengi. Hauta jenga nyumba kwa jina langu, kwasababu umemwaga damu nyingi

kwenye ardhi machoni pangu. 9 Walakini, utapata mwana ambaye atakuwa mtu
wa amani. Nitampa kupumzika na maadui zake kwa kila upande. Kwa kuwa jina
lake litaitwa Sulemani, na nitatoa amani na utulivu kwa Israeli katika siku zake.
10 Ata jenga nyumba kwa jina langu. Ata kuwa mwana wangu, na nitakuwa baba
yake. Nitaimarisha kiti cha enzi cha ufalme wake juu ya Israeli. 11 Sasa, mwanangu,
Yahweh awe nawe na kukuwezesha kufanikiwa. Uweze kujenga nyumba ya Yahweh
Mungu wako, kama alivyo sema utajenga. 12 Yahweh tu akupe uwelewa na ufahamu,
ili utii sheria ya Yahweh Mungu wako, ata kapokuweka kiongozi juu ya Israeli.
13 Kisha utafanikiwa, kama tu ukitii maagizo na amri Yahweh alizo mpa Musa kuhusu
Israeli. Kuwa hodari na mshujaa. Usiogope wala kufadhaika. 14 Sasa, ona, kwa bidii
kubwa nimeandaa kwa ajili ya nyumba ya Yahweh talanta 100, 000 za dhahabu,
talanta milioni moja za fedha, na shaba na chuma katika idadi kubwa. Pia nimetoa
mbao na mawe. Lazima uongeze zaidi katika haya. 15 Una wafanya kazi wengi:
wachonga mawe, maseremala, wanaume wenye ujuzi mbali mbali, 16 wenye uwezo
wa kufanya kazi na dhahabu, fedha, shaba, na nishati. Hivyo anza kufanya kazi,
na Yahweh awe nawe. 17 Daudi akawaagiza viongozi wote Waisraeli wamsaidie
Sulemani mwanae, akisema, 18 "Yahweh Mungu wenu yupo nanyi na amewapa amani
kila pande. Amewakabidhi mikononi mwangu wenyeji wote mkoa. Mkoa umetiishwa
mbele za Yahweh na watu wake. 19 Sasa mtafuteni Yahweh Mungu wenu kwa moyo
wenu wote na nafsi. Simameni na mjenge sehemu takatifu ya Yahweh Mungu. Kisha
mwaweza kuleta sanduku la agano la Yahweh na vitu vya Mungu ndani ya nyumba
iliyo jengwa kwa ajili ya jina la Yahweh.

# 23

1 Daudi alipo kuwa mzee na kukaribia mwisho wa maisha yake, alimfanya
Sulemani mwanae mfalme juu ya Israeli. 2 Aliwakusanya pamoja viongozi wote
wa Israeli, na makuhani na Walawi. 3 Walawi walio kuwa miaka thelathini na
zaidi walihesabiwa. Idadi ya elfu thelathini na nane. 4 Kwa hawa, elfu ishirini
na nne walikuwa kusimamia kazi ya nyumba ya Yahweh, na elfu sita walikuwa
maaskari na waamuzi. 5 Elfu nne walikuwa walinzi wa lango, na elfu nne walikuwa
wamsifu Yahweh na vyombo nilivyo vitengeneza vya kusifu." Daudi akasema.
6 Akawatenganisha kwenye vikundi kulingana na wana wa Levi: Gerishoni, Kohathi,
na Merari. 7 Kwa koo za uzao wa Gerishoni, kulilkuwa na Ladani na Shimei.
8 Palikuwa na watatu wa wana wa Ladani: Yehieli kiongozi, Zethami, na Yoeli.
9 Palikuwa na watatu wa wana wa Shimei: Shelomothi, Hazieli, na Harani. Hawa
walikuwa viongozi wa koo ya Ladani. 10 Palikuwa na wanne wa wana wa Shimei:
Yahathi, Ziza, Yeushi, na Beria. 11 Yahathi alikuwa mkubwa, Ziza wapili, lakini
Yeushi na Beria hawakuwa na wana wengi, hivyo walihesabiwa kama ukoo mmoja
na kupangiwa kazi sawa. 12 Palikuwa na wanne wa wana wa Kohathi: Amramu,
Izhari, Hebroni, na Uzieli. 13 Hawa walikuwa wana wa Amramu: Aruni na Musa.
Aruni alichaguliwa kuandaa vitu vitakatifu, yeye na uzao wake watatoa uvumba
kwa Yahweh, kumtumikia na kumpa baraka kwa jina lake. 14 Lakini kwa Musa mtu
wa Mungu, wana wake walihesabiwa kuwa Walawi. 15 Wana wa Musa walikuwa
Gerishomu na Eliezeri. 16 Uzao wa Gerishomu ulikuwa Shebueli mkubwa. 17 Uzao wa
Eliezeri alikuwa Rehabia. Eliezeri hakuwa na wana wengine, lakini Rehabia alikuwa
na uzao mkubwa. 18 Mwana wa Izihari alikuwa Shelomithi kiongonzi. 19 Uzao wa
Hebroni ulikuwa Yeria, mkubwa, Amaria wapili, Yahazieli watatu, na Yekameamu
wanne. 20 Wana wa Uzieli walikuwa Mika mkubwa, na Ishia wapili. 21 Wana wa
Merari walikuwa Mahili na Mushi. Wana wa Mahili walikuwa Eleazari na Kishi.
22 Eleazari alikufa bila mtoto wa kiume. Alikuwa na mabinti tu. Wana wa Kishi
waliwaoa. 23 Wana wa Mushi watatu walikuwa Mahili, Ederi, na Yeremothi. 24 Hawa

walikuwa uzao wa Lawi kuligana na koo zao. Walikuwa viongozi, wamehesabiwa na
kuorodheshwa kwa majina, kuanzia koo zilizo fanya kazi katika nyumba ya Yahweh,
kutoka miaka ishirini na zaidi. 25 Kwa kuwa Daudi alisema, “Yahweh, Mungu wa
Israeli, amewapa pumziko watu wake. Anafanya makao yake Yerusalemu milele.
26 Walawi hawataitaji kubeba hema la kuabuadia na vifaa vyake vinavyo tumika
kwenye utumishi wake.” 27 Kwa maneno ya Daudi ya mwisho Walawi walihesabiwa,
miaka ishirini na kuendelea. 28 Wajibu wao ulikuwa kuwasaidia wazao wa Aruni
katika utumishi wa nyumba ya Yahweh. Walikuwa washughulikie nyuani, vyumbani,
utakasaji wa vitu vyote vya Yahweh, na kazi zingine katika utumishi wa nyumba ya
Mungu. 29 Pia walishughulikia mkate wa uwepo, unga safi wa mbegu za sadaka,
maandazi ya siotiwa chachu, sadaka za ngano, sadaka ziliochanganywa na mafuta,
na vipimo vyote vya idadi n a ukubwa wa vitu. 30 Pia walisimama kila asubui
kumshukuru na kumsifu Yahweh. Pia walifanya hivi jioni 31 na kila wakati sadaka
ya kuteketezwa ilipo tolewa kwa Yahweh, siku ya Sabato na sherehe za mwezi mpya
na siku za maakuli. Idadi iliyo pangwa, iliyo tolewa kwa amri, ilipaswa kuwa mbele
ya Yahweh. 32 Walikuwa viongozi wa hema la kukutania, patakatifu, na kuwasaidia
ndugu zao wa uzao wa Aruni katika utumishi wa nyumba ya Yahweh.

# 24

1 Makundi vya kazi kulingana na uzao wa Aroni yalikuwa haya: Nadabu,
Abihu, Eleazari na Ithamari. 2 Nadabu na Abihu walikufa kabla ya baba yao
kufa. Walikuwa hawana watoto, kwahiyo Eleazari na Ithamari walitumika kama
makuhani. 3 Daudi pamoja na Zadoki, uzao wa Eleazari, na Ahimeleki, uzao wa
Ithamari, waliwagawanya katika makundi yao ya kazi kama makuhani. 4 Kulikuwa
na wanaume viongozi zaidi kati ya uzao wa Eleazari kuliko kati ya uzao wa Ithamari,
kwahiyo waligawanya uzao wa Eleazari katika makundi kumi na sita. Walifanya
hivyo na viongozi wa ukoo na uzao wa Ithamari. Magawanyo haya yalikuwa nane
kwa idadi, sambamba na koo zao. 5 Waliwagawanya bila upendeleo kwa kura, kwa
kuwa walikuwa waamuzi watakatifu na waamuzi wa Mungu, kutoka pande zote
uzao wa Eleazari na uzao wa Ithamari. 6 Shemaia mwana wa Nethaneli mwandishi,
Mlawi, aliandika majina yao mbele ya mfalme, muamuzi, kuhani Zadoki, Ahimeleki
mwana wa Abiathari, na viongozi wa makuhani na familia za Walawi. Ukoo mmoja
ulichaguliwa kwa kura kutoka uzao wa Eleazari, na kisha uliofata utachaguliwa
kutoka uzao wa Ithhamari. 7 Kura ya kwanza ilienda kwa Yehoiaribu, ya pili kwa
Yedaia, 8 ya tatu kwa Harimu, ya nne kwa Seorimu, 9 ya tano kwa Malikija, ya sita
kwa Mijamini, 10 ya saba kwa Hakozi, ya nane kwa Abija, 11 ya tisa kwa Yeshua, ya
kumi kwa Shekania, 12 ya kumi na moja kwa Eliashibu, ya kumi na mbili kwa Yakimu,
13 ya kumi na tatu kwa Hupa, ya kumi na nne kwa Yesheheabu, 14 ya kumi na tano
kwa Biliga, ya kumi na sita kwa Imma, 15 ya kumi na saba kwa Heziri, ya kumi na
nane kwa Hapizezi, 16 ya kumi na tisa kwa Pethaia, ya ishirini kwa Yehezikeli, 17 ya
ishirini na moja kwa Yakini, ya ishirini na mbili kwa Gamuli, 18 ya ishirini na tatu
kwa Delaia, na ya ishirini na nne kwa Maazia. 19 Hii ilikuwa taratibu ya utumishi
wao, walipo kuja kwenye nyumba ya Yahweh, wakifuata utaratibu waliopewa na
Aruni babu yao, kama Yahweh, Mungu wa Israeli, alivyo waagiza. 20 Hawa walikuwa
Walawi waliobakia: Wana wa Amiramu, Shebueli; wana wa Shebaeli, Yedeia. 21 Wana
wa Rehabia: wana wa Rehabia, Ishia kiongozi. 22 Wa Waizari, Shelomothi; mwana wa
Shelomothi, Yahathi. 23 Wana wa Hebroni: Yeria kiongozi, Amaria wapili, Yahazieli
watatu, na Yekameamu wanne. 24 Wana wa uzao wa Uzieli ulimjumuisha Mika. Uzao
wa Mika ulimjumuisha Shamiri. 25 Kaka wa Mika alikuwa Ishia. Wana wa Ishia
akijumuishwa Zakaria. 26 Wana na Merari: Mahli na Mushi. Mwana wa Yaazia,

Beno. [27] Wana wa Merari: Yaazia, Beno, Shohamu, Zakuri, na Ibrri. [28] Wana wa
Mahili: eleazari, ambaye alikuwa hana wana. [29] Wana wa Kishi: Yerameli [30] wana
wa Mushi: Mahli, Eda, na yerimothi. Walikuwa walawi, walio orodheshwa na familia
zao. [31] Wanaume hawa ambao walikuwa vichwa katika nyumba za baba zao na kila
wadogo zao, walipiga kura katika uwepo wa Mfalme Daudi, na Zadoki na Ahimeleki,
pamoja na viongozi wa familia wa makuhani na Walawi. Walirusha kura kama uzao
wa Aroni walivyofanya.

# 25

[1] Daudi na viongozi wa wafanyakazi wa hema la kuabudia walichaguliwa kwa kazi
baadhi walikuwa wana wa Asafu, Hemani, na Yeduthuni. Wanaume hawa walitabiri
kwa vinubi, vifaa vya uzi, na upatu. Hii ni orodha ya wanaume walioifanya hii kazi:
[2] Kutoka wana wa Asafu: Zakuri, Yosefu, Nethania, na Asharela, wana wa Asafu, chini
ya mwongozo wa Asafu, ambaye alitabiri chini ya uwangalizi wa mfalme. [3] Kutoka
wana wa Yeduthuni: Gedalia, Zeri, Yeshaia, Shimei, Hashabia, na Matithia, sita kwa
ujumla, chini ya mwongozo wa baba yao Yeduthuni, ambaye alipiga kinubi kwa
kutoa shukurani na kumsifu Yahweh. [4] Kutoka wana wa Hemani: Bukia, Matania,
Uzieli, Shebueli, na yerimothi, Hanania, Hanani, Eliatha, Gidalti, Romamti Ezeri,
yoshibekasha, Mallothi, Hothiri, na Mahaziothi. [5] Hawa wote walikuwa wana wa
Hemani mfalme wa manabii. Mungu alimpa Hemani wana kumi na nne na mabinti
watatu kwa ajili ya kumpa heshima. [6] Hawa wote walikuwa chini ya mwongozo
wa baba yao. Walikuwa ni waimbaji katika nyumba ya Yahweh, pamoja na upatu
na vifaa vya uzi walivyohudumu katika nyumba ya Mungu. Asafu, Yeduthuni, na
Hemani walikuwa chini ya uwangalizi wa mfalme. [7] Wao na kaka zao walikuwa
na uwelewa na walifundishwa kutengeneza muziki kwa Yahweh walikuwa na idadi
ya 288. [8] Walirusha kura kwa majukumu yao, wote sawa, sawa kwa vijana na
kwa wazee, kwa walimua na kwa wanafunzi. [9] Sasa kuhusu wana wa Asafu: kura
ya kwanza iliangukia katika familia ya Yusufu; ya pili iliangukia katika familia ya
Gedalia, idadi ya watu kumi na mbili; [10] ya tatu iliangukia kwa Zakuri, wana wake na
ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili; [11] ya nne iliangukia kwa Izri, wana wake
na ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili; [12] ya tano iliangukia kwa Nethania,
wana wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili; [13] ya sita iliangukia kwa
Bukia, wana wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili; [14] ya saba iliangukia
kwa Yesharela, wana wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili; [15] ya nane
iliangukia kwa Yeshaia, wana wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili; [16] ya
tisa iliangukia kwa Matania, wana wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili;
[17] ya kumi iliangukia kwa Shimei, wana wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi na
mbili; [18] ya kumi na moja iliangukia kwa Azareli, wana wake na ndugu zake, idadi
ya watu kumi na mbili; [19] ya kumi na mbili iliangukia kwa Hashabia, wana wake na
ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili; [20] ya kumi na tatu iliangukia kwa Shubaeli,
wana wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili; [21] ya kumi na nne iliangukia
kwa Matithia, wana wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili; [22] ya kumi
na tano iliangukia kwa Yeromothi, wana wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi
na mbili; [23] ya kumi na sita iliangukia kwa Hanania, wana wake na ndugu zake,
idadi ya watu kumi na mbili; [24] ya kumi na saba iliangukia kwa Yoshibekasha, wana
wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili; [25] ya kumi na nane iliangukia
kwa Hanani, wana wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili; [26] ya kumi
na tisa iliangukia kwa Malothi, wana wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi na
mbili; [27] ya ishirini iliangukia kwa Eliatha, wana wake na ndugu zake, idadi ya watu
kumi na mbili; [28] ya ishirini na moja iliangukia kwa Hothiri, wana wake na ndugu

zake, idadi ya watu kumi na mbili; 29 ya ishirini na mbili iliangukia kwa Gidalti, wana
wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili; 30 ya ishirini na tatu iliangukia kwa
Mahaziothi, wana wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi na mbili; 31 ya ishirini
na nne iliangukia kwa Romamti Eza, wana wake na ndugu zake, idadi ya watu kumi
na mbili.

# 26

1 Huu ulikuwa mgawanyiko wa walinzi wa lango: Kutoka kwa Wakora, Meshelemia
mwana wa Kore, wa uzao wa Asafu. 2 Meshelemia alikuwa na wana wa kiume:
Zekaria mzaliwa wa kwanza, Yediaeli wapili, Zebadia watatu, Yathinieli wanne,
3 Elamu watano, Yehohanani wasita, Eliehoenai wasaba. 4 Obedi alikuwa na wana
wa kiume: Shemaia wa kwanza, Yehozabadi wapili, Yoa watatu, na Sakari wanne, na
Nethanieli watano, 5 Amieli wasita, Isakari wasaba, Peulethai wanane, kwa kuwa
Mungu alimbariki Obedi Edomu. 6 Kwa Shemaia mwanae walizawa wana walio
tawala familia zao; walikuwa wanaume wenye uwezo mbali mbali. 7 Wana wa
Shemaia walikuwa Othini, Refaeli, Obedi, na Elizabadi. Ndugu zake Elihu na Semakia
walikuwa wanaume wenye uwezo mbali mbali. 8 Hawa wote walikuwa uzao wa
Obedi Edomu. Wao na wanao na ndugu zao walikuwa wanaume wenye uwezo wa
kufanya wajibu wao katika huduma ya hema la kuabudia. Palikuwa na sitini na mbili
walio kuwa na undugu na Obedi Edomu. 9 Meshelemia alikuwa na wana na ndugu,
wanaume wenye uwezo, jumla ya kumi na nane. 10 Hosa, mzao wa Merari, alikuwa
na wana: Shimiri kiongozi (japo hakuwa mzaliwa wa kwanza, baba yake alimfanya
kiongozi), 11 Hilikia wapili, Tebalia watatu, Zekaria wanne. Wote wa wana wa Hosa na
ndugu walikuwa kumi na tatu kwa idadi. 12 Huu mgawanyiko wa walinzi wa lango,
sambamba na viongozi, ulikuwa na majukumu, kama ndugu zao, kutumika katika
nyumba ya Yahweh. 13 Walirusha kura, wadogo kwa wakubwa, kulingana na familia
zao, kwa kila lango. 14 Kura ilipo rushwa kwa lango la mashariki, ilimuangukia
Shelemia. Kisha wakarusha kura kwa Zekaria mwana wake, mshauri makini, na
kura yake ikatokea lango la kaskazini. 15 Kwa Obedi Edomu kulipangiwa lango la
kusini, na wanae walipangiwa nyumba za ghala. 16 Shufimu na Hosa walipangiwa
lango la magharibi pamoja na lango la Shalekethi, kwa barabara ya juu. Lindo
lilikabiidhiwa kwa kila familia. 17 Kwa mashariki walikuwa Walawi sita, kaskazini
kwa siku moja, kusini kwa siku moja, na nyumba za ghala wawili. 18 Katika ua
kuelekea magharibi wanne walipangwa, wanne barabarani, na wawili katika ua.
19 Haya yalikuwa magawanyiko ya walinzi wa lango. Palijazwa na uzao wa Kora na
Merari. 20 Miongoni mwa Walawi, Ahija alikuwa kiongozi wa hazina ya nyumba ya
Mungu, na hazina ya vitu vya Yahweh. 21 Wazao wa Ladani, walitoka kwa Gerishoni
kupitia kwake na walio kuwa viongozi wa familia za Ladani Mgerishoni, walikuwa
Yehieli na wanae, 22 Zethamu, na Yoeli kaka yake, aliyesimamia ghala za nyumba ya
Yahweh. 23 Kulikuwa na askari walio chukuliwa kwa koo za Amramu, Izhari, Hebroni,
na uzieli. 24 Shebueli mwana wa Gerishomu mwana wa Musa, alikuwa msimamizi
wa nyumba za ghala. 25 Ndugu zake wa ukoo wa Eliezeri walikuwa Rehabia mwanae,
mwana wa Rehabia Yeshaia, mwana wa Yeshaia Yoramu, mwana wa Yoramu Zikiri,
na mwana wa Zikiri Shelomothi. 26 Shelomothi na ndugu zake walikuwa wasimamizi
wa nyumba zote za ghala zinazo hifadhi vitu vyote vya Yahweh, ambavyo Daudi
mfalme, viongozi wa familia, wakuu wa maelfu na mamia, na wakuu wa jeshi
walivyo vitenga. 27 Walitenga vitu walivyo vichukuwa kwenye mapambano kwa ajili
ya kutunza nyumba ya Yahweh. 28 Pia walikuwa wahusika wa kila kitu kilicho tengwa
kwa ajili ya Yahweh na Samweli nabii, Sauli mwana wa Kishi, Abneri mwana wa Neri,
na Yoabu mwana wa Zeruia. Kila kitu kilicho tengwa kwa ajili ya Yahweh kilikuwa
chini ya ulinzi wa shelomothi na ndugu zake. 29 Wa uzao wa Izhari, Kenania na

wana wake walikuwa wahusika wa mambo ya ndani ya Israeli. Walikuwa maafisa
na waamuzi. 30 Wa uzao wa Hebroni, Hashabia na kaka zake, wanaume wenye uwezo
1, 700, walikuwa wahusika wa kazi ya Yahweh na kazi ya mfalme. Walikuwa upande
wa mgharibi mwa Yordani. 31 Kutoka uzao wa Hebroni, Yeriya alikuwa kiongozi wa
uzao wake, walihesabiwa kutoka orodha za familia zao. Katika mwaka wa arobaini
wa utawala wa Daudi walitathimini kumbukumbu na kugundua miongoni mwao
wanaume wa uwezo katika Yazeri ya Gileadi. 32 Yerija alikuwa na ndugu 2, 700,
walio kuwa viongozi wenye uwezo katika familia. Daudi aliwafanya waangalizi wa
makabila ya Rubeni na Gadi, na nusu kabila la Manase, kwa kila jambo linalo muhusu
Mungu, na kwa mambo ya mfalme.

# 27

1 Hii ni orodha ya familia za viongozi wa Israeli, wakuu wa maelfu na mamia,
pamoja na maafisa wa jeshi walio mtumikia mfalme kwa namna tofauti. Kila kikosi
cha jeshi kilitumika mwenzi hadi mwezi kwa mwaka mzima. Kila kikosi kilikuwa
na wanaume elfu ishirini na nne. 2 Kwa mwezi wa kwanza wa kikosi alikuwa
Yashobeamu mwana wa Zabdieli. Katika kikosi chake kulikuwa na wanaume elfu
ishirini na nne. 3 Alikuwa miongoni mwa uzao wa Perezi na mhusika wa maafisa
wa jeshi kwa mwezi wa kwanza. 4 Juu ya kikosi kwa mwezi wa pili alikuwa Dodai,
wa ukoo wa uliotoka kwa Ahoa. Mikilothi alikuwa wa pili kwa cheo. Katika kikosi
chake walikuwa wanaume elfu ishirini na nne. 5 Mkuu wa jeshi wa mwezi wa
tatu alikuwa Benaia mwana wa Yehoiada, kuhani na kiongozi. Katika kikosi chake
walikuwa wanaume elfu ishirini na nne. 6 Huyu ni Benaia aliye kuwa kiongozi wa
wale thelathini na juu ya wale thelathini. Amizabadi mwanae alikuwa katika kikosi
chake. 7 Mkuu kwa mwezi wa nne alikuwa Asaheli kaka wa Yoabu. Zebadia mwanae
akawa mkuu baada yake. Katika kikosi chake kulikuwa na wanaume elfu ishirini na
nne. 8 Mkuu kwa mwezi wa tano alikuwa Shamihuthi, mzao wa Izra. Katika kikosi
chake walikuwa wanaume elfu ishirini na nne. 9 Mkuu kwa mwezi wa sita alikuwa
Ira mwana wa Ikeshi, kutoka Tekoa. Katika kikosi chake walikuwa wanaume elfu
ishirini na nne. 10 Mkuu kwa mwezi wa saba alikuwa Helezi Mpeloni, kutoka watu
wa Efraimu. Katika kikosi chake walikuwa wanaume elfu ishirini na nne. 11 Mkuu
kwa mwezi wa nane alikuwa Sibekai Mhushathi, kutoka ukoo ulitoka kwa Zera.
Katika kikosi chake walikuwa wanaume elfu ishirini na nne. 12 Mkuu kwa mwezi
wa tisa alikuwa Abi Ezeri Manathothi, kutoka kwa kabila la Benjamini. Katika kikosi
chake walikuwa wanaume elfu ishirini na nne. 13 Mkuu kwa mwezi wa kumi alikuwa
Maharai kutoka mji wa Netofa, kutoka ukoo ulio toka kwa Zera. Katika kikosi chake
walikuwa wanaume elfu ishirini na nne. 14 Mkuu kwa mwezi wa kumi na moja
alikuwa Benaia kutoka mji wa Pirathoni, kutoka kabila la Efraimu. Katika kikosi
chake walikuwa wanaume elfu ishirini na nne. 15 Mkuu kwa mwezi wa kumi na mbili
alikuwa Helidai kutoka mji wa Netopafa, kutoka ukoo uliotoka kwa Othinieli. Katika
kikosi chake walikuwa wanaume elfu ishirini na nne. 16 Hawa walikuwa viongozi wa
makabila ya Israeli: Kwa kabila la Rubeni, Eliezeri mwana wa Zikri alikuwa kiongozi.
Kwa kabila la Simeoni, Shefatia mwana wa Maka alikuwa kiongozi. 17 Kwa kabila la
Lawi, Hashinia mwana wa Kemueli alikuwa kiongozi, na Zadoki aliongoza uzao wa
Aruni. 18 Kwa kabila la Yuda, Elihu, mmoja wa kaka zake Daudi, alikuwa kiongozi.
Kwa kabila la Isakari, Omri mwana wa Mikaeli alikuwa kiongozi. 19 Kwa kabila
la Zebuluni, Ishimaia mwana wa Obadia alikuwa kiongozi. Kwa kabila la Naftali,
Yeremothi mwana wa Azirieli alikuwa kiongozi. 20 Kwa kabila la Efraimu, Hoshea
mwana wa Azazia alikuwa kiongozi. Kwa kabila la Manase, Yoeli mwana wa Pedaia
alikuwa kiongozi. 21 Kwa nusu kabila la Manase lililo Gileadi, Ido mwana wa Zekaria
alikuwa kiongozi. Kwa kabila la Benjamini, Yaasieli mwana wa Abneri alikuwa
kiongozi. 22 Kwa kabila la Dani, Azareli mwana wa Yerohamu alikuwa kiongozi.

Hawa walikuwa viongozi wa makabila ya Israeli. 23 Daudi hakuwa hesabu wenye
umri wa miaka ishirini au chini zaidi, kwasababu Yahweh alihaidi kuongeza Israeli
kama nyota za mbinguni. 24 Yoabu mwana wa Zeruia alianza kuhesabu wanaume,
lakini hakumaliza. Gadhabu iliangukia Israeli kwa hili. Hii idadi haikuandikwa
kwenye nyakati za mfalme Daudi. 25 Azimavethi mwana wa Adieli alikuwa mhusika
wa hazina za mfalme. Yonathani mwana wa Uzia alikuwa juu ya nyumba za ghala
katika mashamba, kwenye miji, na vijijini, na kwenye minara iliyo imarishwa. 26 Ezri
mwana wa Kelubi alikuwa juu ya mashamba, hao walio lima ardhi. 27 Shimei kutoka
Rama alikuwa juu ya mashamba ya mizabibu, na Zabdi kutoka Shefamu alikuwa
juu ya mizabibu na mhifadhi wa mvinyo. 28 Mwangalizi wa miti mizeituni na miti ya
mikuyu iliyo kuwa bondeni alikuwa Baali Hanani kutoka Gederi, na juu ya nyumba za
ghala za mafuta alikuwa Yoashi. 29 Juu ya mifugo iliyo kuwa inalishwa huko Sharoni
alikuwa Shitrai kutoka Sharoni, na juu ya mifugo iliyo kuwa mabondeni alikuwa
Shafati mwana wa Adlai. 30 Msimamizi wa ngamia alikuwa Obili Mishimaeli, na juu
ya punda wakike alikuwa Yehideia kutoka Meronothi. Juu ya mifugo alikuwa Yazizi
Mhagri. 31 Hawa wote walikuwa wasimamizi wa mali za Mfalme Daudi. 32 Yonathani,
mjomba wake Daudi alikuwa mshauri, sababu alikuwa na busara na mwandishi.
Yehieli mwana wa Hakimoni aliwajali watoto wa mfalme. 33 Ahithofeli alikuwa
mshauri wa mfalme, na Hushai kutoka watu wa Waariki alikuwa mshauri wake wa
siri. 34 Nafasi ya Ahithofeli ilichukuliwa na Yehoiada mwana wa Benaia, na Abiathari.
Yoabu alikuwa mkuu wa jeshi la mfalme.

# 28

1 Daudi akakusanya waamuzi wote wa Israeli Yerusalemu: waamuzi wa makabila,
maafisa wa vitengo walio mtumikia mfalme katika kazi walizo pangiwa, wakuu wa
maelfu na mamia, wasimamizi wa mali zote za mfalme na mwanae, na maafisa na
wanaume wa mapambano, ukijumuisha wale wenye ujuzi sana. 2 Daudi mfalme
akainuka kwa miguu yake na kusema, “Sikilizeni mimi, kaka zangu na watu wangu.
Ilikuwa dhumuni langu kujenga hekalu kwa ajili ya sanduku la agano la Yahweh;
stuli ya miguu kwa ajili ya Mungu wetu, na nimefanya maandalizi kuijenga. 3 Lakini
Mungu akaniambia, 'Hautajenga hekalu kwa ajili ya jina la langu, kwasababu wewe
ni mwanaume wa vita na umemwaga damu.' 4 Bado Yahweh, Mungu wa Israeli,
alinichagua kutoka katika familia ya baba yangu kuwa mfalme wa Israeli milele.
Amechagua kabila la Yuda kama kiongozi. Katika kabila la Yuda, na nyumba ya
baba yangu, kutoka kwa wana wa baba yangu, amenichagua kuwa mfalme wa
Israeli. 5 Kutoka kwa wana wengi ambao Yahweh amenipa, amemchagua Sulemani,
mwanangu, kuketi katika kiti cha enzi cha ufalme wa Yahweh, juu ya Israeli.
6 Aliniambia, 'Sulemani mwanae atanijengea nyumba yangu na nyuani mwangu, kwa
kuwa nimemchagua kuwa mwana wangu, nami nitakuwa baba yake. 7 Nitaimarisha
ufalme wake, akidumu kutii sheria na amri zangu, kama ulivyo siku ya leo.' 8 Kisha
sasa, katika macho ya Waisraeli wote, ili kusanyiko la yahweh, na katika uwepo wa
Mungu wetu, nyinyi nyote lazima mshike na kufanya amri zote za Yahweh Mungu
wenu. Fanyeni hivi ili mmiliki nchi nzuri na kuacha urithi wa watoto wenu baada
yenu milele. 9 Kwako wewe, Sulemani mwanangu, mtii Mungu wa baba yako,
mtumikie kwa moyo wako wote na roho ya utayari. Fanya hivi kwasababu yahweh
anachunguza mioyo yote na kufahamu amasa ya kila wazo la mtu. Ukimtafuta,
ataonekana kwako, lakini ukimtelekeza, atakukataa milele. 10 Elewa kuwa Yahweh
amekuchagua kujenga hekalu ili kama sehemu yake takatifu. Kuwa imara na
ufanye.” 11 Kisha Daudi akamkabidhi Sulemani mwanae mipango ya baraza la
hekalu, jengo la hekalu, vyumba vya hifadhi, vyumba vya juu, vyumba vya ndani, na

chumba chenye mfuniko wa maombezi. 12 Alimpatia mipango aliyo chora ya nyuani
kwa ajili ya nyumba ya Yahweh, vyumba vyote vilivyo zunguka, vyumba vya hifadhi
katika nyumba ya Mungu, na hazina za vitu vya Yahweh. 13 Alimpatia masharti kwa
vitengo vya makuhani na Walawi, kwa majukumu walio pangiwa katika nyumba ya
Yahweh, na kwa vyombo vyote vinavyo tumika katika nyumba ya Yahweh. 14 Alimpa
uzito wote wa vifaa vya dhahabu kwa kila huduma na vifaa vyote vya fedha, na
vitu vyote kwa kila namna ya huduma. 15 Haya maelekezo yalitolewa kwa uzito,
ukijumuisha maelekezo yote ya vinara vya taa vya dhahabu na taa za dhahabu,
maelekezo kwa uzito kwa kila vinara vya taa, kwa vinara vya taa vya fedha, na
maelekezo kwa matumizi sahihi ya vinara vya taa vyote. 16 Alitoa uzito wa dhahabu
kwa meza za mkate wa uwepo, kwa kila meza, na uzito wa fedha kwa meza za fedha.
17 Alitoa uzito wa dhahabu safi kwa uma za nyama, bakuli, na vikombe. Alitoa uzito
kwa kila bakuli ya dhahabu, na uzito kwa kila bakuli ya fedha. 18 Alitoa uzito wa
dhahabu ya kutakasika kwa madhabahu ya uvumba, na kwa dhahabu kwa ajili ya
mchoro wa makerubi waliye tanda mabawa yao na kufunika sanduku la agano la
Yahweh. 19 Daudi akasema, “ Nimeeka haya katika maandishi kama Yahweh alivyo
ni elekeza na kunipa kuelewa kuhusu mchoro.” 20 Daudi akasema kwa Sulemani
mwanae, “Kuwa hodari na mjasiri. Fanya kazi. Usiogope au kuwa na wasiwasi, kwa
kuwa Yahweh Mungu, Mungu wangu, yupo nawe. Hatakuacha wala kukutelekeza
mpaka kazi ya huduma ya hekalu la Yahweh imekamilika. 21 Ona, hivi ni vitengo
vya makuhani na Walawi kwa huduma katika hekalu la Mungu. Watakuwa nawe,
pamoja na wanaume walio tayari na wenye ujuzi, kukusaidia katika kazi na kutenda
huduma. Waamuzi na watu wote wako tayari kufuata amri zako.”

# 29

1 Mfalme Daudi akasema kwa kusanyiko lote, “Sulemani mwanangu, ambaye
mwenyewe Mungu amemchagu, bado nimdogo na hana uzoefu, na jukumu ni kubwa.
Maana hekalu sio kwa ajili ya watu bali la Mungu. 2 Hivyo nimefanya kwa ubora
wangu kutoa kwa ajili ya hekalu la Mungu. Nina toa dhahabu kwa vitu vya kujengwa
na dhahabu, fedha kwa vitu vya kujengwa na fedha, shaba kwa vitu vya kujengwa na
shaba, nishati kwa vitu vya kujengwa na nishati, na mbao kwa vitu vya kujengwa na
mbao. Pia nina toa mawe ya shohamu, mawe ya kupangwa, mawe ya upambaji
wandani ya rangi mbali mbali - kila haina ya mawe ya thamani - na marimari
kwa wingi. 3 Sasa, kwasababu ya mapenzi yangu kwa nyumba ya Mungu, Ninatoa
hazina yangu binafsi ya dhahabu na fedha. Ninafanya hivi kwa nyongeza kwa yote
niliyofanya katika hekalu takatifu: 4 talanta za dhahabu elfu tatu kutoka Ofiri, na
talanta elfu saba za fedha zilizotakasika, ili kufunika kuta za majengo. 5 Ninachangia
dhahabu kwa vitu vya kujengwa na dhahabu, na fedha kwa vitu vya kujengwa na
fedha, na kazi zote zinazotakiwa kufanywa na wajenzi. Nani mwingine anataka
kuchangia kwa Yahweh leo na kujitoa kwake?” 6 Kisha sadaka za hiari zilitolewa
na viongozi wa mababu wa familia zao, viongozi wa makabila ya Israeli, wakuu
wa maelfu na mamia, na waamuzi waliojuu ya kazi ya mfalme. 7 Walitoa kwa
ajili ya huduma ya nyumba ya Mungu talanta elfu tano na darkoni elfu kumi za
dhahabu, talanta elfu kumi za fedha, talanta elfu nane za fedha, na talanta za chuma
100, 000. 8 Haao walio na mawe ya thamani waliyatoa katika Hazina ya nyumba
Yahweh, chini ya usimamizi wa Yehieli, mzao wa Gerishoni. 9 Watu walifurahi kwa
ajili ya hizi sadaka za hiari, kwasababu walitoa kwa moyo wao wote kwa Yahweh.
Mfalme Daudi pia alifurahi sana. 10 Daudi alimbariki Yahweh mbele ya kusanyiko
lote. Alisema, “Na uabudiwe, Yahweh, Mungu wa Israeli babu wetu, milele na milele.
11 Kwako, Yahweh, kuna ukuu, nguvu, utukufu, ushindi, na enzi. Kwa kuwa yote

yalio mbinguni na duniani ni yako. Kwako ni ufalme, Yahweh, na umetukuzwa
kama mtawala juu ya vyote. [12] Utajiri na heshima utoka kwako, unatawala juu
ya watu wote. Mkononi mwako kuna nguvu na uwezo. Unao uweza na nguvu ya
kuwafanya watu kuwa mkuu na kumpa uweza yeyote. [13] Kisha sasa, Mungu wetu,
tunakushukuru na kusifu jina lako tukufu. [14] Lakini mimi ni nani, na watu wangu
ni nani, tustahili kutoa kwa hiari hivi vitu? Kweli, vitu vyote vya toka kwako, na
tumerudisha kwako vilivyo vyako. [15] Kwa kuwa sisi ni wageni na wasafiri mbele
zako, mababu zetu wote walikuwa. Siku zetu katika dunia ni kama kivuli, na hakuna
tumaini la kubaki duniani. [16] Yahweh Mungu wetu, utajiri wote tulio kusanya kujenga
hekalu kwa kuheshimu jina lako - watoka kwako na ni wako. [17] Ninajua, Mungu
wangu, unachunguza moyo na wapendezwa na unyofu. Kwangu mimi, kwa unyofu
wa moyo wangu nimetoa kwa hiari vitu vyote, na sasa natazama kwa furaha watu
walio hapa wakitoa tunu kwako. [18] yahweh, Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Israeli -
mababu zetu - hifadhi hili katika fikra za watu wako. Elekeza mioyo yao kwako.
[19] Mjalie Sulemani mwanangu moyo wa shauku wakutii amri zako, shuhuda za
agano lako, na maagizo yako, na kutekeleza mipango hii yote ya kujenga nyumba
niliyoiandaa." [20] Daudi akasema kwa kusanyiko lote, "Sasa mbariki Yahweh Mungu
wenu." Kusanyiko lote likambariki Yahweh, Munug wa mababu zao, wakainamisha
vichwa vyao na kumuabudu Yahweh na kusujudu mbele za mfalme. [21] Kwa siku
iliyo fuata, wakatoa dhabiu kwa Yahweh na kumtolea sadaka ya kuteketeza. Walitoa
sadaka ya ng'ombe elfu moja, kondoo elfu moja, na wana kondoo elfu moja, pamoja
na sadaka zao za vinywaji na dhabihu tele kwa Israeli yote. [22] Siku ile, walikunywa
na kula mbele za Yahweh kwa furaha tele. Walimfanya Sulemani, mwana wa Daudi,
mfalme mara ya pili, na kumpaka mafuta ya mamlaka ya Yahweh kuwa mfalme. Pia
walimpaka Zadoki mafuta kuwa mfalme. [23] Kisha Sulemani akaketi kwenye kiti cha
enzi cha Yahweh kama mfalme baada ya Daudi baba yake. Alifanikiwa, na Israeli
yote ikamtii. [24] Viongozi wote, wanajeshi, na Mfalme Daudi wanae wakaonyesha
utii kwa Mfalme Sulemani. [25] Yahweh alimheshimu sana Sulemani na kumkirimia
nguvu kubwa kuliko mfalme yeyote aliyetangulia kabla yake Israeli. [26] Daudi mwana
wa Yese alitawala Israeli yote. [27] Daudi alikuwa mfalme wa Israeli kwa miaka
arobaini. Alitawala kwa miaka saba Hebroni na miaka thelathini na tatu Yerusalemu.
[28] Alikufa katika umri mzuri mkubwa, baada ya kufurahia maisha marefu, utajiri na
heshima. Sulemani mwanae alitawala baada yake. [29] Mafanikio ya mfalme Daudi
yameandikwa katika historia ya Samweli nabii, katika historia ya Nathani nabii, na
katika historia ya Gadi nabii. [30] Yalio ekwa kwenye kumbukumbu ni matendo ya
utawala wake, mafanikio yake na mambo yalio mdhuru, Israeli, na falme zote za
nchi zingine.

# 2 Mambo ya Nyakati

1 Selemani mwana wa Daudi, aliimariswa katika utawala wake, na Yahwe Mungu
wake alikuwa pamoja naye na alimpa nguvu nyingi sana. 2 Sulemani akasema
kwa Isralei wote, na maakida wa maelfu na wa mamia, na kwa waamuzi, na kwa
kila mfalme kiongozi katika Israeli yote, wakuu wa kaya. 3 Hivyo Sulemani na
kusanyiko lote wakaenda pamoja naye sehemu ya juu iliyokuwa Gibeoni, maana
ndipo palikuwepo hema ya kukutania ya Mungu, ambayo Musa mtumishi wa Yahwe,
alikuwa ameitengeneza jangwani. 4 Lakini Daudi alikuwa ameleta pale sanduku la
Mungu kutoka Kiriath yeriam hadi sehemu ambayo alikuwa ametayarisha, maana
alikuwa ameliandalia hema huko katika Yerusalemu. 5 Zaidi ya hayo, madhabahu
ya shaba iliyotengenezwa na Bezaleli mwana wa uri mwana wa Huri ilikuwepo
huko kabla ya mbele ya madhabahu ya Yahwe; Sulemani na kusanyiko wakaenda
ilikokuwa. (Maandiko ya zamani yanasema 6 Selemani akaenda huko kwenye kwenye
madhabahu ya shaba mbele za Yahwe, ambayo ilikuwepo mahali pa hema ya
kukutamia, na akatoa sadaka elfu za kuteketezwa juu yake. 7 Mungu akamtokea
Selemani usiku huo na akasema kwake, “Omba! Nikupe nini?” 8 Selemani akasema
kwa Mungu, “Umeonesha agano la uaminifu mkuu kwa Daudi baba yangu, na
umenifanya mfalme katika nafasi yaye. 9 Sasa, Yahwe Mungu, ahadi yako kwa Daudi
baba yangu itimie, maana umenifanya mfalme juu ya watu wengi kama mavumbi
ya dunia. 10 Sasa nipe hekima na maarifa, ili niweze kuwaongoza watu hawa,
maana ni nani anayeweza kuwaamua watu wako, ambao ni wengi sana kwa idadi?”
11 Mungu akasema kwa Selemani, “Kwa kuwa hili lilikuwa kwenye moyo wako, na
kwa kuwa hujaomba mali, utajiri, au heshima, wala maisha ya wale wanaokuchukia,
wala maish marefu kwa jili yako binafsi, lakini umeomba hekima na maarifa kwa
ajili yako, ili uwatawale watu wangu, ambao juu yao nimekufanya mfame, na hivi
ndivyo nitafanya. 12 Sasa nitakupa hekima na maarifa, pia nitakupa mali na utajiri,
na heshima, kuliko wafalme wote waliokuwepo kabla yako walivyokuwa, na baada
yako hakuna yeyote atakayekuwa navyo.” 13 Kwa hiyo Selemani akaenda Yerusalemu
kutoka sehemu ya juu iliyokuwepo Gibeoni, kutoka mbele ya hema ya kukutania;
akatawala juu ya Israeli. 14 Selemani akakusanya magari na wanaume waendesha
farasi, naye alikuwa na magari 1, 400 na waendesha farasi kumi na mbili elfu
ambao aliwaweka katika miji ya magari, pamoja naye, mfalme katika Yerusalemu.
15 Mfalme akatengeneza fedha na dhahabu kuwa vitu vya kawaida kama mawe katika
Yerusalemu, na mbao za mierezi kuwa kama miti ya mikuyu iliyomo katika nyanda
za chini. 16 Selemani katika uagizaji wa farasi kutoka Misiri, wafanya biashara wake
walinunua farasi kutoka Misiri kwa bei stahiki. 17 Waliagiza gari kutoka Misiri kwa
shekeli mia sita za fedha, na farasi mmoja kwa shekeli 150. Pia walinunua kutoka
kwa wafalme wa Wahiti na wafalme wa Washamu.

## 2

1 Sasa Selemani akaamuru kulijengea nyumba jina la Yahwe na nyumamba kwa
ajili ya ikulu ya ufalme wake. 2 Selemeni akateua wanaume elfu sabini wabebe
mizigo, na wanaume elfu themanini wa kukata mbao katika mlima, na wanaume
3, 600 kwa ajili ya kusimamia. 3 Selemani akatuma ujumbe kwa Hiramu, mfalme
wa Tiro, ukisema, “Kama ulivyofanya na Daudi baba yangu, ulivyomtumia magogo
ya mierezi ili ajenge nyumba ya kuishi, fanya hivyo hivyo na mimi. 4 Tazama, niko
karibu kujenga nyumba kwa ajili ya jina la Yahwe Mungu wangu, kuiweka wakifu

kwake, kwa ajili ya kumtolea sadaka za kuteketezwa zenye viungo vitamu mbele
zake, kwa ajili ya mkate wa uwepo, na kwa ajili ya sadaka za kuteketezwa asubuhi
na jioni, katika siku za Sabato na za mwezi mpya, na katika sikukuu zilizoteuliwa
kwa ajili ya Yahwe Mungu wetu. Hii itakuwa milele, kwa Israeli. 5 Nyumba
nitakayoijenga itakuwa kubwa sana, maana Mungu wetu ni mkuu kuliko miungu
mingine yote. 6 Lakini ni nani anayeweza kumjengea Mungu nyumba, kama dunia
yote na hata mbigu yenyewe haviwezi kumtosha? Mimi ni nani hata nimjengee
nyumba, ispokuwa sadaka kwa ajili ya sadaka za kufukiza mbele zake? 7 Kwa hiyo
nileteeni mtu mwenye ujuzi wa kazi katika kazi ya dhahabu, fedha, shaba, na chuma,
na ya dhambarau, na nyekundu, na sufu ya samawati, mtu anayejua kutengeza
aina zote za mapambo ya mbao. Atakuwa na watu wenye ustadi waliopamoja
nami katika Yuda na Yerusalemu, ambao Daudi baba yangu aliwaweka. 8 Nitumieni
pia mierezi, miberoshi, na miti ya msandali kutoka Lebanoni, maana najua ya
kuwa watumishi wako wanajua jinsi ya kukata mbao katika Lebanoni. Angalia,
watumishi wangu watakuwa na watumishi wako, 9 ili kwamba watayarishe mbao
nyingi kwa ajili yangu, maana nyumba ninayotaka kuijenga itakuwa kubwa na ya
ajabu. 10 Angalia, nitawapa watumishi wako, watu watakaozikata mbao, kori ishirini
elfu za ngano ya aridhini, kori ishirini elfu za shayiri, bathi ishirini elfu za mvinyo,
na bathi ishirini elfu za mafuta." (Maandishsi ya kale yanasema: "kori ishirini
elfu za ngano kama chakula"). 11 Kisha Hiramu, mfalme wa Tiro, akajibu kwa
maandishi, ambayo alimtumia Selemani: "Kwa kuwa Yahwe anawapenda watu wake,
amekufanya kuwa mfalme juu yao." 12 Zaidi ya hayo, Hiramu akasema, "Abarikiwe
Yahwe, Mungu wa Israeli, aliyeziumba mbingu na dunia, amempa Daudi mwana
mwenye hekima, mwenye karama ya busara na uelewa, ambaye atajenga nyumba
kwa aajili ya Yahwe, na nyumba kwa ajili ya ufalme wake. 13 Sasa nimemtum
mtu mwenye ujuzi, mwenye karama ya uelewa, Hiramu, mtaalamu wangu. 14 Ni
mwana wa mwanamke wa binti za Dani. Baba yake alikuwa mtu kutoka Tiro.
Ana ujuzi katika kazi za dhahabu, fedha, shaba, chuma, mawe, na katika mbao,
na katika dhambarau, samawati, na sufu yenkundu, na kitani safi. Pia ana ujuzi
katika kutengeneza michoro ya aina yoyote na katika kubuni kitu chochote. Apatiwe
nafsi miongoni mwa watumishi wako wenye ujuzi, na pamoja na wale wa bwana
wangu, Daudi, baba yako. 15 Sasa, ngano na shayiri, mafuta na mvinyo, ambayo
bwana wangu aliisema, na apeleke sasa vitu hivi kwa watumishi wake. 16 Tutakata
mbao kutoka Lebanoni, mbao nyingi kadri unavyohitaji. Tutazileta kwako kama
mitumbwi kupitia bahari kwenda Yafa, na utazibeba hadi Yerusalemu." 17 Selemani
akawahesabu watu wageni waliokuwa katika nchi ya Israeli, kwa kutumia njia ya
Daudi, baba yake, aliyoitumia kuwahesabu. Walikutwa wako 153, 600. 18 Miongoni
mwao aliwateua sabini elfu ili wabebe mizigo, themanini elfu kuwa wakataji wa
mbao katika milima, na 3, 600 kuwa wasimamizi wa kuwasimamia watu wafanye
kazi.

# 3

1 Kisha Selemani akaanza kuijenga nyumba ya Yahwe katika Yerusalemu juu
ya Mlima Moria, ambako Yahwe alimtokea Daudi baba yake. Aliandaa sehemu
ambayo Daudi aliikusudia, katika sakafu ya kupuria ya Arauna Myebusi. 2 Alianza
kujenga siku ya pili ya mwezi wa pili, katika mwaka wa nne wa utawala wake.
3 Sasa hivi ndinyo vipimo vya ule msingi ambao Selemani alijenga kwa ajili ya
nyumba ya Mungu. Akitumia mtindo wa vipimo vya zamani, urefu ulikuwa mikono
sitini, na upana ulikuwa mikono ishirini. 4 Urefu wa ukumbi mbele ya nyumba
ulikuwa mikono ishirini, ukilingana na upana wa nyumba, urefu wake kwenda

juu pia ulikuwa mikono ishirini, na Selemani akaifunika sehemu ya ndani kwa
dhahabu halisi. [5] Akailitengeneza paa la ukumbi mkuu kwa miti ya miberoshi,
ambayo aliifunika kwa dhahabu halisi, na ambayo aliifunika kwa miti ya mitende
na minyororo. [6] Akaipamba nyumba kwa vito vya thamani; dhahabu ilikuwa
dhahabu kutoka Parvaimu. [7] Pia akazifunika boriti zake, vizingiti, kuta, na milango
kwa dhahabu; akachonga makerubi juu ya kuta zake. [8] Akaijenga sehemu ya
patakatifu pa patakatifu. Urefu wake ulilingana na upana wa nyumba, mikono
ishirini, na upana wake pia ulikuwa mikono ishirini. Aliifunika kwa dhahabu halisi,
thamani yake ilikuwa talanta mia sita. [9] Uzito wa misumari ulikuwa shekeli hamsini
za dhahabu. Alizifunika sehemu za juu kwa dhahabu. [10] Akachonga makerubi
wawili kwa ajili ya sehemu za patakatifu pa patakatifu, wahunzi wakayafunika
kwa dhahabu. (Maandishi ya kale yanasema: makerubi wawili waliochongwa
kwenye mbao). [11] Mabawa ya makerubi yalikuwa na urefu wa mikono ishirini
yote kwa pamoja; bawa la kerubi mmoja lilikuwa na urefu wa mikono mitano,
lilifikia kwenye ukuta wa chumba; bawa jingine lilikuwa na urefu wa mikono mitano
pia. [12] Bawa la kerubi mwingine lilikuwa mikono mitano, likifikia kwenye ukuta
wa chumba; bawa lake jingine lilikuwa mikono mitano pia, likigusana na bawa la
kerubi wa kwanza. [13] Mabawa ya makerubi hawa yalienea jumla ya mikono mitano.
Makerubi yalisimama kwa miguu yake, na nyuso zake zikiuelekea ukumbi mkuu.
[14] Akatengeneza pazia la samawati, dhambarau, na sufu nyekundu, na kitani safi, na
akachora makerubi juu yake. [15] Selemani pia akatengeneza nguzo mbili, kila moja
ikiwa na urefu wa mikono thelathini na tano kwenda juu, kwa maana mbele ya
nyumba; taji ambazo zilikuwa juu ya nguzo zilikuwa na urefu wa mikono mitano
kwenda juu. [16] Akatengeneza minyororo kwa ajili ya nguzo na akaiweka juu yake,
pia akatengeneza maakomamanga mia moja na akayaunganisha kwenye minyororo.
[17] Akazisimamisha nguzo mbele ya hekalu, mkono wa kulia, na nyingine mkono wa
kushoto; akaiita nguzo ya kulia Yakini, na nguzo ya kushoto akaiita Boazi.

# 4

[1] Vivile akatengeneza madhabahu ya shaba; urefu wake ulikuwa mikono ishirini,
na upana wake ulikuwa mikono ishirini. [2] Pia akatengeneza bahari ya mduara ya
chuma cha kuyeyushwa, mikono kumi kutoka ukingo hadi ukingo. Urefu wake
kwenda juu ulikuwa mikono mitano, na bahari ilikuwa na mzunguko wa mikono
thelatinini. [3] Chini ya kingo kuzunguka bahari kulikuwapo ng'ombe dume, kumi
kila mkono, [4] Bahari ilisimama juu ya ng'ombe wa kulima kumi na wawili, watatu
wakiangalia kaskazini, watatu wakiangalia magharibi, na watatu wakiangalia kusini,
na watatu wakiangalia mashariki. Bahari iliwekwa juu yao, na robo ya sehemu zao
za nyuma zote zilikuwa ndani. [5] Bahari ilikuwa nene kama upana wa mkono, na
ukingo wake ulikuwa kama ukingo wa kikombe, kama ua la yungi. Bahari ilikuwa na
mabafu elfu tatu ya maji. [6] Pia akatengeneza birika kumi kwa ajili ya kuoshea vitu;
tano akaziweka mkono wa kulia, na tano akaziweka kushoto; vifaa vilivyotumika
katika kufanayia sadaka za kuteketezwa zilipaswa kuoshwa ndani ya hizo birika.
Bahari, vilevile ilikuwa kwa ajili ya makauhani kuoga humo. [7] Akatengeza vinara
vya taa kumi vya dhahabu ambavyo vilitengenezwa kutokana na maelekezo ya jinsi
vilivyopaswa kuwa; akaviweka hekaluni, vitanao mkno wa kulia, na vitano mkono
wa kushoto. [8] Akatengeneza meza kumi na kuziweka hekaluni, tano upande wa
kulia, na tano upande wa kushoto. Akatengeneza birika mia moja za dhahabu.
[9] Zaidi ya hayo akatengeneza mahakama ya makuhani na mahakama kuu, na milangu
kwa ajili ya mahakama, akaifunika milango yake kwa shaba. [10] Akaiweka bahari
upande wa kulia wa nyumba, masharika, ikielekea upande wa kusini. [11] Huramu

akayatengeza masufuria, majembe, na mabakuli ya kunyunyizia. Hivyo Huramu
akamaliza kazi aliyofanya kwa ajili ya mfalme Selemani katika nyumba ya Mungu:
12 zile nguzo mbili, taji mfano wa upinde zilizo kuwa juu ya zile nguzo mbili, na
nyavu mbili za za mapambo zilizofunika zile taji mbili mfano wa upinde zilizokuwa
juu ya zile nguzo. 13 Alikuwa ametengeneza makomamanga mia nne kwa ajili ya
zile nyavu za mapambo: safu mbili za makomamanga kwa kila wavu ili kufunika
vimbe mbili zilizo kuwa juu ya nguzo. 14 Pia akavitengeneza vitako na mabirika
juu ya kitako, 15 bahari moja na wale ng'ombe kumi na wawili chini yake, 16 pia
masufuria, majembe, nyuma za nyama, na vyombo vingine vyote. Huramu mtaalamu
akavifanya kwa ajili ya Mfalme Selemani, kwa ajili ya nyumba ya Yahwe, vya shaba
iliyong'arishwa. 17 Mfalme alikuwa amevisubu katika uwanda wa Yordani, katika
udongo wa mfinyanzi kati kati ya Sukothi na Sereda. 18 Hivyo ndivyo Selemani
alivyovitengeneza vyombo vyote kwa wingi; kwa kweli, uzito wa shaba haukuweza
kujulikana. 19 Selemani akazitengeza samani zote ambazo zilikuwa kwenye nyumba
ya Mungu, pia madhabahu ya dhahabu, na meza ambazo juu yake mkate wa uwepo
ulipaswa kuwekwa; 20 vinara pamoja na taa zake, ambazo zilitengezwa ili kumulika
mbele ya chumba cha ndani—hivi vilitengenezwa kwa dhahabu halisi; 21 na maua,
taa, na makoleo, ya dhahabu, dhahabu safi. 22 Pia mikasi ya taa, na mabakuli,
vijiko, na vikaango vya sadaka za kuteketezwa vyote vilitengenezwa kwa dhahabu
safi. Kuhusu mlanago wa kuingilia kwenye nyumba, milango yake ya ndani kwenye
patakatifu pa patakatifu na milango ya nyumba, ambayo ni, ya hekalu, ilitengenezwa
kwa dhahabu.

# 5

1 Wakati ilipomalizika kazi aliyofanya Selemani kwa ajili ya Yahwe, Selemani
akapeleka vitu ndani, ambavyo Daudi, baba yake, aliviweka wakifu kwa kusudi
hilo, pamoja na zile fedha, dhahabu, na vyombo vyote akavileta ndani ya hazina
ya nyumba ya Mungu. 2 Kisha Selemanai akawakusanya wazee wa Israeli, wakuu
wa makabila yote, na viongozi wa familia za watu wa Israeli, katika Yerusalemu,
ili walilete sanduku la agano la Yahwe kutoka mji wa Daudi, ambao ni Sayuni.
3 Wanaume wote wa Israeli wakakusanyika mbele za mfalme katika sikukuu, ambayo
ilikuwa katika mwezi wa saba. 4 Wazee wote wa Israeli wakaja, na Walawi
wakalichukua sanduku. 5 Wakalileta sanduku, hema ya kukutania, na vyombo
vitakatifu vyote ambavyo vilikuwa ndani ya hema. Makuhani waliokuwa wa kabila
la Lawi wakavileta vtu hivyo. 6 Mfalme Selemanai na kusanyiko lote la Israeli
wakaja pamoja, mbele ya sanduku, wakitoa sadaka za kondoo na maksai ambao
hawakuweza kuhesabika. 7 Makuhani wakalileta sanduku la anago la Yahwe ndani
mahali pake, katika chumba cha ndani cha nyumba, kwenye patakatifu pa patakatifu,
chini ya mabawa ya makerubi. 8 Kwa kuwa makerubi walitandaza mabawa yao
juu ya mahali pa sanduku, na walilifunika sanduku na na miti yake ya kulibebea.
9 Miti ilikuwa mirefu sana kwamba ncha zake zlionekana kutoka ile sehemu takatifu
mbele ya chumba cha andani, lakini hazikuweza kuonekana kutoka nje. Zipo hapo
hadi leo. 10 Hapakuwa na kitu katika sanaduku isipokuwa zile meza mbili ambazo
Musa aliziweka humo huko Horebu, wakati Mungu alipofanya agano na watu wa
Israeli, walipotoka nje ya Misri. 11 Ilikuwa makuhani walipotoka nje ya sehemu
takatifu. Makuhanai wote wliokuwepo wakajiweka wakifu wenyewe kwa Yahwe,
bila kujiamuru wenyewe kulingana na sehemu zao. 12 Pia makuhani waliokuwa
waimbaji, wote kwa ujumla wao, pamoja na Asafu, Hemani, Yeduthuni, na wana
wao na ndugu zao, wakiwa wamevalia kitani safi na wakipiga matoazi, vinanda, na
vinubi, wakaasimama upande wa mashariki wa mwisho wa madhabahu. Pamoja

nao palikuwa na makuhuni 120 wakipuliza tarumbeta. 13 Ikawa kwamba wapuruza
tarumbeta na waimbaji wakafanya mziki pamoja, wakifanya sauti moja isikike kwa
ajili ya kumsifu na kumshukuru Yahwe. Walipaza sauti zao kwa tarumbeta, toazi na
vyombo vingine, na wakamsifu Yahwe. Wakaimba, "Kwa maana Yeye ni mwema,
kwa kuwa uaminifu wa agano lake wadumu milele." Kisha nyumba, ile nyumba ya
Yahwe, ikajawa na wingu. 14 Makuhani hawakuweza kusimama ili wahudumu kwa
sababu ya lile wingu, kwa maana utukufu wa Yahwe uliijaza nyumba yake.

# 6

1 Kisha Selemani akasema, "Yahwe alisema kwamba ataishi katika giza nene,
2 lakini nimekujengea makao makuu, sehemu kwa ajili yako ya kuishi milele." 3 Kisha
mfaalme akageuka nyuma na kuwabariki kusanyiko lote la Israeli, wakati kusanyiko
lote la Israeli walikuwa wamesimama. 4 Akasema, "Yahwe, Mungu wa Israeli,
usifiwe, uliyesema na Daudi baba yangu, na ametimiza kwa mikono yake mwenyewe,
akisema. 5 'Tangu siku nilipowaleta watu wanagu nje ya nchi ya Misiri, sikuchaagua
mji wowote nje ya makabaila yote ya Israeli ambamo nyumba ingejengwa, ili jina
lanagu liwe humo. Wala sikuchagua mtu yeyote kuwa mfalme juu ya watu wangu
Israeli. 6 Aidha, nimechagua Yeruselemu, ili kwamba jina langu liwe humo, na
nimemchagua Daudi kuwa juu ya watu wanagu Israeli. ' 7 Sasa ilikuwa ndani ya
moyo wa Daudi baba yangu, kujenga nyumba kwa ajili ya jina la Yahwe, Mungu wa
Israeli. 8 Lakini Yahwe alisema kwa Daudi Baba yanagu. 'Kwmba ilikuwa ndani ya
moyo wako kujenga nyumba kwa ajili ya jina langu, ulifanya vizuri kwa hili kuliweka
moyono mwako. 9 Aidha, hutaijenga ile nyumba, badala yake, mwanao, mmoja
atakayetoka kwenye viuno vyako, ataijenga nyumba kwa ajili ya jina langu.' 10 Yahwe
ameyatimiza maneno aliyokuwa amesema, kwa maana nimeiinua sehemu ya Daudi
baba yangu, na ninkaa juu ya kiti cha enzi cha Israeli, kama alivyoahidi Yahwe.
Nimeijenga nyumba kwa ajii ya jina la Yahwe, Mungu wa Israeli. 11 Nimeliweka
humo sanduku, amabamo kuna agano la Yahwe, alilofanya na watu wa Israeli."
12 Selemani akasimama mbele ya madhabahu ya Yahwe mbele za kusanyiko lote la
Israeli, na akanyosha mikono yake. 13 Kwa mana alikuwa ametengeneza jukwaa la
shaba, lenye urefu wa mikono mitano, upana wa mikono mitano, urefu wake kwenda
juu mikono mitatu. Alikuwa ameliweka katika ya uwanja. Akasimama juu yake na
kupiga magoti mbele ya kusanyiko la Israeli, kisha akanyosha mikono yake kuzielekea
mbingu. 14 Akasema, "Yahwe, Mungu wa Israeli, hakuna Mungu kama wewe katika
mbingu, au juu ya dunia, ambaye anatunza agano na upendo imara na watumishi
wako ambao hutembea mbele zako kwa moyo wao wote; 15 wewe uliyetimtimizia
Daudi baba yanagu, uliyokuwa umemwahidi. Ndiyo, ulisema kwa kinywa chako na
umetimiza kwa mkono wako, kama ilivyo leo. 16 Sasa, Yahwe, Mungu wa Israeli, tunza
ahadi uliyoahidi kwa mtumishi wako Daudi baba yangu, uliposema, 'Hautashindwa
kupata mtu mbele yangu wa kukaa juu ya kiti cha enzi cha Israeli, ikiwa tu uzao wako
ni waangalifu kutembea katika sheria yangu, kama wewe ulivyotembea mbele zangu.
17 Sasa, Mungu wa Israeli, ninaomba kwamba ahadi uliyofanya kwa mtumishi wako
Daudi itakuwa kweli. 18 Lakini kweli Mungu ataishi na wanadamu juu ya dunia?
Angalia, dunia yoye na mbugu yenyewe haviwezi kukubeba -sembuse na hekalu
hili nililojenga! 19 Nakusihi yaheshimu maombi haya ya mtumishi wako na ombi
lake. Yahwe Mungu wangu; sikia kilio na amaombi ambayo mtumishi wako anaomba
mbele zako. 20 Fumbua macho yako kuelekea hekaalu hili usiku na mchana, sehemu
aambaayo uliahidi kuliweka jina lako. Nakuomba usikie maombi atakayoomba
mtumishi wako kuelekea sehemu hii. 21 Hivyo sikia maombi ya mtumishi na ya
watu wako Israeli tunapoomba kuelekea sehemu hii. Ndiyo, sikia kutoka mahali

unapoishi, kutoka mbinguni; na unaposikia, samehe. [22] Kama mtu atamtenda dhambi
jirani yake na ikampasa kuapa kiapo, na ikiwa atakuja na kuapa kiapo mbele ya
madhabahu yako katika nyumba hii, [23] basi sikia kutoka mbinguni na kutend na
ukawahukumu watumishi wako, ukamlipizie mwovu, ili kuyaleta matendo yake juu
ya kichwa chake. Ukamtangaze mwenye haki kuwa hana hatia, ili kumlipa thawabu
kwa ajili ya uaminifu wake. [24] Watu wako watakaposhindwa na adui kwa sababu
wamekutenda dhambi, kama watageuka nyuma kwako, wakilikili jina lako, wakisali
na kuomba msamaha mbele zako hekaluni— [25] basi tafadhali sikia mbinguni na
usamehe dhambi za watu wako Isaraeli; uwarudishe katika nchi uliyoitoa kwa ajili
yao na baba zao. [26] Wakati mbingu zimefungwa na hakuna mvua kwa sababu
watu wamekutenda dhambi—ikiwa wataomba kuelekea sehemu hii, wakilikili jina
lako, na kuziacha dhambi zao utakapokuwa umewaadhibu— [27] basi sikia mbinguni
na usamehe dhambi za watumishi wako na watu wako Israeli, utakapowaelekeza
kwenye njia njema iwapasayo kutembea. Tuma mvua juu ya nchi yako, ambayo
umewapa watu wako kama urithi. [28] Kama kuna njaa katika nchi, au kama kuna
ugonjwa, tauni au ukungu, nzige au viwavijeshi, au kama adui wake wameyavamia
malango ya mji katika nchi yao, au kwamba kuna pigo lolote au ugonjwa— [29] na
ikiwa sala na maombi yamefanywa na mtu au watu wako wote Israel—kila mmoja
akilijua pigo na huzuni katika moyo wake akinyosha mikono yake kuelekea hekalu
hili. [30] Basi sikiliza mbinguni, sehemu ambayo unaishi; samehe, na umlipe kila
mtu kwa njia zake zote; uhaujua moyo wake, kwa sababu wewe na ni wewe pekee
unaijua mioyo ya wanadamu. [31] Fanya hivyo ili kwamba wakuogope wewe, ili
waweze kutembea katika katika njia zako siku zote ambazo wataishi katika nchi
uliyowapa baba zetu. [32] Kwa mgeni ambaye siyo sehemu ya watu wako Israeli,
lakini ambaye- kwa sababu ya ukuu wa jina lako, mkono wako wenye nguvu, na
mkono wako ulionyoshwa- akija na kuomba kuelekea sehemu nyumba hii, [33] basi
sikiliza mbinguni, sehemu ambayo unaishi, na fanya yote ambayo mgeni atakuomba,
ili kwamba watu wote wa dunia walijue jina lako na kukuogopa wewe, kama
wafanyavyo watu wako Israeli, na kwamba waweze kujua kwamba nyumba hii
niliyoijenga inaitwa kwa jina lako. [34] Ikiwa kwamba watu wako wakaenda nje
kupigana dhidi ya adui zao, kwa njia yoyote amabayo unaweza kuwatuma, na
ikiwa kwamba wakaomba kwako kuelekea mji huu ambao umeuchagua, na kuelekea
nyumba ambayo nimeijenga kwa ajili ya jina lako. [35] Basi sikiliza maombi yao
mbinguni, ombi lao, na uwasaidie. [36] Kama wametenda dhambi dhidi yako—kwa
kuwa hakuna asiye tenda dhambi—na ikiwa una hasira nao na kuwakabidhi kwa
adui zao, ili kwamba adui wakawabeba na kuwachukua kama mateka kwa ajili
ya nchi zao, iwe mbali au karibu. [37] Kisha wakatambua kuwa wako katika nchi
ambako wamewekwa utumwani, na ikiwa watatubu na kutafuta msaada kwako
katika utumwa wao. ikiwa watasema, 'Tumetenda kinyume na kutenda dhambi.
Tumetenda kwa uovu,' [38] ikiwa watarudi kwako kwa mioyo yao yote na kwa nia
yao yote katika nchi ya utumwa wao, ambako walichuliwa kama mateka, na ikiwa
wataomba kukabili nchi yao, uliyowapa babu zao, na kukabili mji ambao uliuchagua
na kukabili nyumba ambayo niliijenga kwa ajili ya jina lako. [39] Basi sika kutoka
mbinguni, mahali unapoishi, sikia kuomba kwao na maombi na wayaombayo, na
uwasaidie shida zao. Wasamehe watu wako, ambao wamekutenda dhambi. [40] Sasa,
Mungu wangu, ninakusihi, uyafungue macho yako, na masikio yako yasiskie maombi
yatakayofanywa katika sehemu hii. [41] Sasa basi, amka, Yahwe Mungu, kwenye mahali
pako pa kupumzikia, Wewe na sanduku la nguvu zako. Makuhani wako, Yahwe
Mungu, wavikwe wokovu, na watakatifu wako wafurahi katika wema. [42] Yahwe
Mungu, usiugeuze nyuma uso wa masihi wako. Yakumbuke matendo yako katika

agano lako la ufalme kwa ajili ya Daudi, mtumishi wako.

# 7

1 Sasa Selemani alipokuwa amemaliza kuomba, moto ukaja kutoka mbinguni na
kuiteketeza sadaka ya kuteketezwa na dhabihu, na utukufu wa Yahwe ukaijaza
nyumba. 2 Makuhani hawakuweza kuingia kwenye nyumba ya Yahwe, kwa sababu
utukufu wake uliijaza nyumba yake. 3 Watu wote wa Israeli wakaangalia juu moto
uliposhuka chini na utukufu wa Yahwe ulikuwa juu ya nyumba. Wakalala kwa nyuso
zao juu ya sakafu ya mawe, wakaabudu, na kutoa shukrani kwa Yahwe. Wakasema,
"Kwa maana yeye ni mwema, kwa maana agano lake la kifame ladumu milele."
4 Kwa hiyo mfalme na watu wote wakamtolea Yahwe sadaka Yahwe. 5 Mfalme
Selemani akatoa sadaka ya ng'ombe ishirini na mbili elfu na kondoo 120, 000 na
mbuzi. Kwa hiyo mfalme na watu wote wakaiweka wakifu nyumba ya Mungu.
6 Makuhani wakasimama, kila mmoja akasimama mahali pake pa kuhudumu; Walawi
pia pamoja na vyombo vya muziki vya Yahwe, ambavyo mfalme Daudi alivitengeza
kwa ajili ya kumpa shukrani Yahwe katika nyimbo, "Kwa maana uaminifu wa agano
lake wadumu milele." Makuhani wote wakapiga matarumbeta mbele yao, na Israeli
wote wakasimama. 7 Selemani akaitakasa sehemu ya katikati ya kiwanja cha mfalme
mbele ya nyumba ya Yahwe. Humo akatoa sadaka za kuteketezwa na mafuta ya
sadaka za amani, kwa sababu madhabahu ya shaba ambayo alikuwa ametengeza
haikuweza kuzibeba sadaka, sadaka za nafaka, na za mafuta. 8 Kwa hiyo Selemani
akaitisha sikukuu wakati huo kwa siku saba, na Israeli wote pamaoja naye, kusanyiko
kubwa, kutoka Lebo Hamathi mpaka kijito cha Misiri. 9 Siku ya nane wakaitisha
kusanyiko la makini, kwa maana kwa siku saba walishika kuwekwa wakfu kwa
ile madhabahu. 10 Katika siku ya ishini na tatu ya mwezi wa saba, Selemani
akawatanya watu kwenda kwenye nyumba zao kwa furaha na mioyo ya shangwe kwa
sababu ya wema aliokuwa ameuonesha Yahwe kwa Daudi, Selemani, Israeli, na watu
wake. 11 Hivyo Selemani akaimaliza nyumba ya Yahwe na nyumba yake mwenyewe.
Kila kitu kilichokuja katika moyo wa Selemani kwa ajili ya kukitengeneza katika
nyumba ya mfalme na katika nyumba yake mwenyewe, alikitimiza kwa mafanikio.
12 Yahwe akamtokea Selemani usiku na kusema kwake, "Nimesikia maombi yako,
na nimeichagua sehemu hii kwa ajili yangu mwenyewe kama nyumba ya dhabihu.
13 Kama nitazifunga mbingu ili kwamba kusiwepo mvua, au kama nitaamuru nzige
waimeze nchi, au kama nitatuma magonjwa kati kati ya watu wangu, 14 kisha watu
wangu, ambao wameitwa kwa jina langu, watajinyenyekeza, kuomba, kuutafuta
uso wangu, na kuziacha njia zao mbaya, nitasikia kutoka mbinguni, kuwasamehe
dhambi zao, na kuiponya nchi yao. 15 Sasa macho yangu yatakuwa wazi na masikio
yangu yatasikiliza maombi yanayofanywa katika sehemu hii. 16 Kwa maana sasa
nimeichagua na kauitakasa nyumba hii ili kwamba jina langu lipate kuwa humo
milele. Masikio yangu na moyo wangu vitakuwako kila siku. 17 Kwako wewe,
kama utatembe mbele zangu kama baba yako Daudi alivyotembea, ukitii yote
nilyokuamuru na kuzishika sheria zangu na maagizo yangu, 18 basi nitakithibitisha
kiti cha enzi cha ufalme wako, kama nilivyosema katika agano na Daudi baba
yako, niliposema, 'Mzaliwa wako hatashindwa kamwe kuwa mtawala katika Israeli.'
19 Lakin ukigeuka, na kuzisahau sheria zangu na amri amabzo nimeweka mbele yenu,
na kama utaenda kuabudu miungu wengine na kuwasujudia, 20 basi nitawang'oa
kutoka kwenye nchi yangu amabayo nimewapa. Nyumba hii ambayo nimeitakasa
kwa ajili ya jina langu, nitaitupilia mbali kutoka mbele zangu, na nitaifanya kuwa
methali na utani miongini mwa watu wote. 21 Ingawa hekalu hili hili zuri sana kwa
sasa, kila mtu apitaye karibu yake atashangazwa na ataguna. Watauliza, 'Kwa nini

Yahwe ameifanyia hivi nchi hii na nyumba hii', 22 wengine watajibu, 'Kwa sababu
walimsahau Yahwe, Mungu wao, ambaye alikuwa amewatoa babu zao nje ya nchi ya
Misiri, na wakashikamana na miungu wengine na kuwainamia chini na kuwaabudu.
Hii ndiyo maana Yahwe ameleta majanga haya yote juu yao”

# 8

1 Ikawa karibu ya mwisho wa miaka ishirini, kipindi ambacho Selemani alikuwa
ameijenga nyumba ya Yahwe na ya kwake mwenye, 2 kwamba Selemani akaiajenga
miji ambayo Hiramu alikuwa amempa, na ndani yake akawaweka watu wa Israeli.
3 Selemani akauavamia Hamathzoba, akaushinda. 4 Akaijenga Tadmori katika nyika,
na miji yote ya hazina, ambayo aliijenga katika Hamathi. 5 Pia akaujenga Beth-
horoni wa juu, na Beth-horoni wa chini, miji iliyozungushiwa kwa ukuta, malango,
na makomeo. 6 Akaujenga Baalathi na miji yote ya hazina aliyoimiliki, na miji yote
kwa ajili ya magari yake na miji kwa ajili ya wapanda farasi wake, na chochote
alichotamani kujenga kwa ajili ya starehe zake katika Yerusalemu, katika Lebanoni,
na katika nchi zote zilizokuwa chini ya utawala wake. 7 Kuhusu watu wengine
wote ambao walikuwa wamesalia wa Wahiti, Waamori, Waperizi, Wahivi, Wayebusi,
ambao hawakuwa wa Israeli, 8 watoto wao ambao waliachwa baada yao katika
nchi, ambaoa watu wa Israeli hawakuwaangamiza—Selemani akawafanyisha kazi
kwa nguvu, ndivyo walivyo hata leo. 9 Vile vile, Selemani hakuwafanyisha kazi
kwa nguvu watu wa Israeli. Badala yake, wakawa wanajeshsi wake, maakida wake,
wakuu wake, na maakida wa magari ya majeshi yake na wapanda farasi wake. 10 Pia
hawa walikuwa wakuu wa wakuu wakisimamia wasimamizi waliokuwa wa mfalme
Selemani, walikuwa 250, waliowasimamia watu walioifanya kazi. 11 Selemani
akamleta binti Farao nje ya mji wa Daudi kwenye nyumba aaliyokuwa amemjengea,
kwa maana alisema, “Mke wangu lazima asiishi kataika nyumba ya Daudi mfalme wa
Israeli, kwa sababu kila linapokuja sanduku la Yahwe ni takatifu”. 12 Kisha Selemani
akatoa sadaka za kuteketezwa juu ya madhabahu yake ambayo alikuwa ametengeza
mbele ya ukumbi. 13 Akatoa sadaka kama ilivyohitaka katika ratiba ya kila siku;
akazitoa, kwa kufuata maelekezo yaliyokuwa katika amari ya Musa, katika siku za
Sabato, miezi mipya, na katika siku zilizopangwa mara tatu kila mwaka: Sikukuu ya
mikate isiyochachwa, sikukuu ya majuma, na sikuku ya vibanda. 14 Katika kuyatunza
maagizo ya baba yake Daudi, Selemani akayapanga makundi ya makuhani kwenye
kazi yao, na Walawi kwenye nafasi zao, ili kumsisfu Mungu na kuhudumu mbele
za makuhani, kama ilivyotakiwa katika ratiba ya kila siku. Pia akawateua walinda
lango kwa zamu zao kwa kila lango, kwa maana Daudi, mtu wa Mungu, alikuwa
ameagiza hivyo pia. 15 Watu hawa hawakupotea kutoka kwenye amri ya mfalme kwa
makuhani na Walawi kuhusu jambo lolote, au kuhusu vyumba vya hazina. 16 Kazi
yote aliyoagizwa na Selemani ikakamilika, kutoka siku msingi wa nyumba ya Yahwe
ulipowekwa hadi ilipokamilika. Nyumba ya Yahwe ikamalizika. 17 Kisha Selemani
akaenda Esion geberi, na Elothi, juu ya pwani katika nchi ya Edomu. 18 Hiramu
akatuma meli zake kupitia watumishi wake ambao walikuwa wana maji wenye
uzoefu. Wakasafiri na Selemani na watumishi wa Semani hadi Ofiri. Wakachukua
kutoka huko talanta 450 za dhahabu ambazo walimletea Selemani.

# 9

1 Malikia wa Sheba aliposikia kuhusu umaarufu wa Selemani, akaja Yerusalemu
kumjaribu kwa maswali magumu. Akaja pamoja na msafara mkubwa sana, pamoja
na ngamia waliosheheni manukato, dhahabu nyingi, na vito vingi vya thamani.
Alipofika kwa 2 Selemani, akamwambia yaliyokuwa moyoni mwake. Selemani
akamjibu maswaali yake yote; hakuna kitu kilichokuwa kigumu sana kwa Selemani;

hakuna swali ambalo hakulijibu. 3 Malikia wa Sheba alipoiona hekima ya Selemani
na ikulu aliyokuwa amejenga, 4 chakula mezani kwake, mahali pa kukaa watumishi
wake, kazi ya watumisshi wake na mavazi yao, pia wabebakikombe na mavazi yao,
na namna alivyotoa sadaka za kuteketezwa katika nyumba ya Yahwe, hapakuwa na
roho zaidi ndani yake. 5 Akasema kwa mfalme, “Ni kweli, taarifa ninioisikia katika
nchi yangu kuhusu maneno yako na hekima yako. 6 Sikuamini nilichokisikia mpaka
nilipokuja hapa, na sasa macho yangu yamekiona. Sikuambiwa nusu kuhusu hekima
yako na utajiri wako! Umeuzidi umaarufu niliokuwa nimesikia kuhusu wewe.
7 Wamebarikiwa watu wako, na watumishi wako ambao husimama mbele yako, kwa
sababu wanaisikia hekima yako. (Baadhi ya maandiko yanasema, “Wambarikiwa
wake zako”, ikidhaniwa kwamba kifungu hicho kinapaswa kusomeka kama ilivyo
katika Wafalme 10: 8). 8 Amebarikiwa Yahwe Mungu wako, ambaye amepata raha
ndani yako, aliyekuweka juu ya kiti chake cha enzi, ili uwe mfalme kwa ajili ya Yahwe
Mungu wako. Kwa sababu Mungu wako inaipenda Israeli, ili kuwathibisha milele,
amekufanya kuwa mfalme juu yao, ili ufanye hukumu na haki. 9 Akampa mfalme
talanta 120 za dhahabu na kiasi kikubwa manukato na vit vya thamani. Selemani
hakupewa tena kiasi kikubwa cha manukato kama hiki amabacho alipewa na
malakia wa Sheba. 10 Watumishi wa Hiramau na wa mfalme Selemani, ambaye alileta
dhahabu kutoka Ofiri, miti ya msandali,, na vito vya thamani. 11 Kwa miti hiyo ya
msandali, mfalme Selemani akatengeneza madari ya nyumba ya Yahwe na nyumba
yake, na vinubi na vinanda kwa ajili ya wanamziki. Hapajaonekana tena mbao
kama hiyo katika nchi ya Yuda. 12 Mfalme Selemani akampa malkia wa Sheba kila
kitu alichotaka, chochote alichoomba, zaidi ya vile alivyoleta kwa mfalme Selemani.
Kwa hiyo akaondoka na kurudi kwenye nchi yake, yeye na wataumishsi wake.
13 Sasa uzito wa dhahabu ambayo ililetwa kwa Selemani ndani ya mwaka mmoja
ulikuwa talanta 666 za dhahabu, 14 nje na dhahabu ambayo waliileta wachukuzi na
wafanya biashara. Walme wote wa Arabuni na maliwali katika nchi pia wakamletea
Selemanai dhahabu na fedha. 15 Mfalme Selemani akatengeneza ngao kubwa mia
mbili za dhahabu iliyofuliwa. Shekeli mia sita za dhahabu zikatumika kwa kila ngao.
16 Pia akatengeneza ngao mia tatu za shahabu iliyopigwa. Minas tatu za dhahabu
zikaenda kwa kila ngao; mfalme akaziweka kwenye ikulu ya Msitu wa Lebanoni.
17 Kisha mfalme atengeneza kiti cha enzi kikubwa cha pembe na kufunika kwa
dhahabu safi. 18 Kulikuwa na ngazi sita kwenda kwenye kiti cha enzi, na sehemu
ya juu ya kiti cha enzi ilikuwa duara. Kulikuwa na mikono kila upande wa kiti,
na simba wawili wamesimama pembeni na hiyo mikono. 19 Simba kumi na wawili
walisimama juu ya zile ngazi, mmoja kila upande wa ngazi sita. 20 Hapakuwa na kiti
cha enzi kama hicho katika ufalme wowote mwingine. Vikombe vyote vya kunywea
vya Selemani vilikuwa vya dhahabu, na vikombe vyote vya mfalme katika Nyumba
ya Msitu wa Lebanoni vilikuwa vya dhahabu halisi. Hakuna hata kimoja kilichokuwa
cha fedha kwa sababu fedha haikuchuliwa kuwa ya thamani katika siku za Selemani.
21 Mfalme alikuwa na meli zilizosafiri baharini, pamoja na meli za Hiramu. Mara
moja kwa mwaka meli zilileta dhahabu, fedha, na pembe, na manukato, na pia
nyani na tausi. 22 Kwa hiyo Mfalme Selemani aliawazidi utajiri na hekima wafalme
wote wa dunia. 23 Dunia yote waliutafuta uwepo wa Selemanai ili kusikia hekima
yake, ambayo Mungu alikuwa ameiweka katika moyo wake. 24 Waliomtembelea
walileta kodi, vyombo vya shaba na dhahabu, nguo, silaha, na manukato, na farasi na
anyumbu, mwaka baada ya mwaka. 25 Selemani alikuwa na mazizi elfu nne kwa ajili
ya farasi na magari, na wapanda farasi kumi na mbili elfu, ambao waliwaweka katika
miji ya magari na pamoja naye katika Yerusalemu. 26 Akatawala juu ya wafalme wote
kutoka mto Efrati hadi nchi ya Wafilisti, na hadi mpaka wa Misiri. 27 Mfalme alikuwa

na fedha katika Yerusalemu, nyingi kama mawe juu ya aridhi. Akazifanya mbao za
mierezi kuwa nyingi kama miti ya mikuyu ambayo iko nyanda za chini. [28] Wakaleta
farasi kutoka Misri na kutoka nchi zote kwa ajili ya Selemani. [29] Kwa mambo mengine
kuhusu Selemani, mwanzo na mwisho, hayajandikwa katika Historia ya Nathani
Nabii, katika unabii wa Abiya Mshinoni, na katika Maono ya Ido mwonaji wa mambo
ya Yeroboamu mwana wa Nabati? [30] Selemani akatawala katika Yerusalemu juu ya
Israeli yote kwa miaka arobaini. [31] Akalala na babu zake na watu wakamzika katika
mji wa Daudi baba yake. Rehoboamu, mwanaye, akawa mfalme katika sehemu yake.

# 10

[1] Rehoboamu akaenda Shekemu, kwa maana Isaraeli wote walikuwa wanakauja
Shekemu kwa ajili ya kumfanya yeye mfalme. [2] Ikatokea kwamba Yeroboamu
mwana wa Nebati akasikia haya (kwa maana alikuwa katika Misiri, ambako alikuw
amekimbilia kutoka kwenye uwepo wa Mfalme Selemanai, lakini Yeroboamu akarudi
kutoka Misiri). [3] Kwa hiyo wakatuma na kumuita yeye, na Yeroboamu na Israeli
wote wakaja; wakamwambia Rehoboamu na kusema, [4] “Baba yako aliifanya nira
yetu ngumu. Kwa hiyo sasa, ifanye kazi ngumu ya baba yako kuwa rahisi, na
ifanye nyepesi nira yako ambayo baba yako aliiweka juu yetu, na sisi tutakutumikia
wewe.” [5] Rehoboamu akawaambia, “Njoni kwangu tena baada ya siku tatu.”
Kwa hiyo watu wakaondoka. [6] Mfalme Rehoboamu akaomba ushauri kwa wazee
ambao walikuwa wamesimama mbele ya Selemani baba yake wakati alipokuwa
hai; akasema, Mnanishauri niwape jibu gani watu hawa?” [7] Wakasema kwake,
Ikiwa wewe ni mwema kwa watu hawa na uwapendeze, na sema maneno mazuri
kwao, basi siku zote watakuwa watumishi wako.” [8] Lakini Rehoboamu akapuuza
ushauri wa wazee ambao walimpa, na akashauriana na wanauame vijana ambao
walikuwa wa rika lake, ambao walisimama mbele yake. [9] Akawaamabia, “Mnanipa
ushauri gani, ili kwamba niwajibu watu waliozungumza kwangu na kusema, “Ifanye
nyepesi nira yako ambayo baba yako aliiweka juu yetu'?” [10] Wanaume vijana
mabaoa walikuwa rika la Yeroboamu wakasema kwake, wakisema, “Hivi ndivyo
utakavyosema kwa watu waliokuambia kwamba baba yako Selemani aliifanya nira
yao nzito, lakini kwamba lazima uifanye nyepesi. Hivi ndivyo utakavyosema kwao,
'Kidole changu kidogo ni kinene kuliko kiuno cha baba yangu. [11] Kwa hiyo sasa,
ingawa babab yangu aliwatwika nira nzito, nitaiongeza nira yenu. Baba yangu
aliwaadhibu kwa mijeredi, lakini nitawaadhibu kwa nge.” [12] Kwa hiyo Yeroboamu
na watu wote wakaja kwa Rehoboamu katika siku ya tatu, kama aliavyosema
mfalme, “Rudini kwangu katika siku ya tatu,” [13] Yeroboamu akasema kwa kwao
kwa ukatili, akiupuuza aushauri wa wazee. [14] Akasema kwao akiufuata ushauri
wa wanaume vijana, akisema, “ Baba yangu aliifanya nira yenu nzito, lakini mimi
nitaiongeza. Baba yangu aliwaadhibu kwa mijeredi, lakini mimi nitawaadhibu kwa
nge.” [15] Kwa hiyo mfalme hakuwasikiliza watu, kwa kuwa lilikuw tukio lililoletwa
na Mungu, kwamba Yahwe aweze kulitimiza neno lake ambalo Ahiya Mshiloni
alikuwa amemwambia Yeroboamu mwana wa Nebati. [16] Israeli wote, walipoona
kwamba mfalme hakuwasikiliza, watu wakamjibu na kusema, “Tunasehemu gani
katika Daudi? Hatuna urith katika wana wa Yese! Kila mmoja wenu anapaswa
kwenda katika hema yake, Israeli. Sasa kila mtu aone nyumba yake, Daudi.” Kwa
hiyo Israeli wote wakarudi kwenye hema zao. [17] Lakini kwa watu wa Yuda walioishi
katika miji ya Yuda, Yeroboamu akatawala juu yao. [18] Kisha mfalme Rehoboamu
akamtuma Adoramu, ambaye alikuwa msimamizi wa wafanya kazi, lakini watu wa
Israeli walimuua kwa kumpiga mawe. Mfalame Rehoboamu akaingia haraka ndani

ya gari lake kwenda Yerusalemu. 19 Kwa hiyo Israeli wakawa waasi dhidi ya nyumba
ya Mungu hadi leo.

# 11

1 Rehoroboamu alipofiki Yerusalemu, akawakusanya nyumba ya Yuda na
Benyamini, wanaume 180, 000 walaiaochaguliwa amabao wliakuwa wanajeshi, kwa
ajili ya kupigana dhiidi ya Israeli, ili kuurudisha ufalme kwa Rehoboamu. 2 Lakini
neno la Yahwe likamjia Shemaya mtu wa Mungu, likisema, 3 "Sema kwa Rehoboamu
mwana wa Selemani, mfalme wa Yuda, na kwa Israeli kataika Yuda na Benyamaini,
4 Yahwe anasema hivi, "Msivamie wala kufanya vita dhidi ya ndugu zako. Kila
mmoja lazima arudi kwenye nyumba yake, kwa maana nimesababisha jambo hili
kutokea." Kwa hiyo wakayatii maneno ya Yahwe na kuacha kumvamia Yeroboamu.
5 Yeroboamu akaishi katika Yerusalemu na kujenga miji katika Yuda kwa ajili ya
kujilinda. 6 Akaijenga Bethelehemu, EtamuTekoa, 7 Bethsusi, Soko, Adulamu, 8 Gathi,
Maresha, Zifu, 9 Adoraimu, Lakishi, Azeka, 10 Sora, Aiyaloni, na Hebroni. Hii ni miji
yenye ngome katika Yuda na Benyamini. 11 Akaziimarisha ngome na kuweka maamri
jeshsi ndani yake, pamaoja na hazina ya chakula, mafuta, na divai. 12 Akaweka ngao
na mikuki katika miji yote na kuifanya imara sana. Kwa hiyo Yuda na Benyamini
zikawa zake. 13 Makuhani na Walawi waliokuwa katika Israeli yote wakaenda kwake
kutoka ndani ya mipaka yao. 14 Kwa kuwa Walawi waliacha nchi za malisho yao
na mali zao ili kuja Yuda na Yerusalemu, kwa maana 15 Yeroboamu na wanaaye
walikuwa wamewafukuza, ili kwamba wasifanye majukumu yao ya kikuhani kwa
ajili ya sehemu za juu na mbuzi na sanamu za ndama alizokuwa ametengeneza.
16 Watu kutoka kabila zote za Israeli wakaja nyuma yao, wale walio wameiilekeza
mioyo yao kumtafuta Yahwe, Mungu wa Israeli; wakaja Yerusalemu kwa ajili ya
kumtolea dhabihu Yahwe. Mungu wa baba zao. 17 Kwa hiyo wakauimarisha ufalame
wa Yuda na kumfanya imara Rehoboamu mwana wa Selemani kwa miaka mitatu,
na wakatembea kwa miaka mitatu katika njia ya Daudi na Selemani. 18 Rehoboamu
akajitwalia mke: Mahalathi, binti wa Yerimothi, mwana wa Daudi na wa Abihaili,
binti wa Eliabu, mwana wa Yese. 19 Akamzalia wana: Yeushi, Shemaraia, na Zahamu.
20 Baaad ya Mahalathi, Rehoboamu akamchukua Maaka, binti Absalomu; akamzalia
Abiya, Atai, Ziza, na Shelomithi. 21 Rehoboamu akampenda Maaka, binti Solomoni,
zaidi kuliko wake za wengine wote na masuria (alichukua wake kumi na nane
na masuria sitini, na akawa baba wa wana ishirini na nane na mabinti sitini).
22 Rehoboamu akamteua Abiya mwana wa Maaka kuwa mkuu, kiongozi miongoni
mwa ndugu zake alikuwa na wazo la kumfanya mfalme. 23 Rehoboamu akatawala
kwa hekima; akawatawanya wanaye katika nchi yote ya Yuda na Benyamini katika
kila mji imara. Pia akawapa chakula kwa wingi na akatafuta wake wengi kwa ajili
yao.

# 12

1 Ikawa kwamba, Rehoboamu alipokuwa ameimarishwa na mwenye nguvu,
kwamba akaikataa sheria ya Yahwe—na Waisraeli wote pamoja naye. 2 Ilitokea
katika mwaka wa tano wa Mfalme Rehoboamu, kwamba, Shishaki, mfalme wa
Israeli, akaja kinyume na Yerusalelemu, kwa sababu watu walikuwa wameacha kuwa
waaminifu kwa Yahwe. 3 Akaja na magari elfu moja na mia mbili pamoja naye
na wapand farasi elfu sitini. Askari wasio hesabika wakaja pamaoja naye kutoka
Misri: Walubi, Wasukii, na Waethiopia. 4 Akaiteka miji yenye ngome ya Yuda na
akaja Yerusalemu. 5 Sasa Shemaya nabii akaja kwa Rehoboamu na kwa viongozi wa
Yuda ambao walikuwa wamekusanyika pamoja Yerusalemu kwa sababu ya Shishaki.
Shemaya akasema kwao, "Hivi ndivyo anavyosema Yahwe: Mmenisahau, kwa hiyo

pia nimewaweka katika mkono wa Shishaki". [6] Kisha wakuu wa Israeli na mfalme
wakajinyenyekeza na kusema, "Yahwe ni mtakatifu." [7] Yaahwe alipoona kuwa
wamejinyenyekeza, neno la Yahwe likamjia Shemaya, likisema, "Wamejinyenyekeza.
Stawaadhibu; nitawaokoa kwa hataua fulani, na hasira yangu haitamiminwa juu
ya Yerusalemu kwa mkono wa Shishaki. [8] Vile vile, watakuwa watumishi wake,
ili kwamba wajue nini maana ya kunitumikia mimi na kuwatumikia watawala
wa nchi zingine." [9] Kwa hiyo Shishaki, mfalme wa Misiri akaja Yerusalemu
akazichukua hazina katika nyumba ya Yahwe, na hazina katika nyumba ya mfalme.
akachukua kila kitu; pia akazichukua ngao za dhahabu alizokuwa amezitengeneza
Selemani. Mfalme [10] Rehoboamu akatengeneza ngao za shaba katika nafasi zake
na kuzikabidhi mikoni mwa maamrijeshi wa walinzi, amabao waliilinda milango ya
kuelekea kwenye nyumba ya mfalme. [11] Ikawa kwamba mfalme kila alipoingia katika
nyumba ya Yahwe, walinzi wakazibeba; kisha wakazirudisha katika nyumba ya
ulinzi. [12] Rehoboamu alipojinyenyekeza mwenyewe, ghadhabu ya Yahwe ikampisha
mbali, kwa hiyo hakumwangamiza kabisa kabisa; pembeni, bado kulikuwa na baadhi
ya wema wa kupatikana katika Yuda. [13] Hivyo mfalme Rehoboamu akafanya ufalme
wake imara katika Yerusalemu, na kwa hiyo akatawala. Rehoboamu alikuwa na
umri wa miaka aroabaini na moja alipoanza kutawala, na akatawala kwa muda
wa mika kumi na saba katika Yerusalemu, mji ambao Yahwe alikuwa ameuchagua
kutoka kwa makabila ya Israeli ili kwamba aliweke jina lake humo. Jina lake aliitwa
Naama, Mwamoni. [14] Akafanya yaliyokuwa uovu, kwa sababu hakuuelekeza moyo
wake kumtafuta Yahwe. [15] Kwa mambo mengine kuhusu Rehoboamu, mwanzo na
mwisho, hayakuandikwa katika maandishi ya Shemaya nabii na ya Ido mwonaji,
ambayo pia yana kumbukumbu ya vizazi na vita kati ya Rehoboamu na Yeroboamu?
[16] Rehoboamu akalala pamoja na babu zake na alizikwa katika mji wa Daudi; Abiya
mwanye akawa mfalme katika nafasi yake.

# 13

[1] Katika mwaka wa kumi na nane wa Mfalme Yeroboamu, Abiya akaanza kutawala
juu ya Yuda. [2] Akatawala kwa miaka mitatu katika Yerusalemu; jina la mama
yake aliitwa Maaka, binti wa Urieli wa Gibea. Kulikuwa na vita kati ya Abiya na
Yeroboamu. [3] Abiya akaingia vitani na jeshi la askari, wenye nguvu, hodari, 400, 00
wanaume waliochaguliwa. Yeroboamu akapanga mistari ya vita dhidi yake yenye
800, 00 wanaume askari waliochaguliwa, wenye nguvu, hodari. [4] Abiya akasimama
juu ya mlima Semaraimu, uliopo katika kilima cha nchi ya Efraimu, na akasema,
"Nisikilizeni, Yeroboamu na Israeli wote! [5] Hamjui kwamba Yahwe, Mungu wa Israeli,
alitoa sheria juu ya Israeli kwa Daudi milele, kwake na kwa wanaye kwa agano
rasimi? [6] Bado Yeroboamu mwana wa Nebati, mtumishi wa Selemani mwana wa
Daudi, akainuka na kuasi dhidi ya bwana wake. [7] Watu wabaya, washirika wa karibu,
wakamkusanyikia, wakamjia kinyume Rehoboamu mwana wa Selemani, wakati
Rehoboamu alipokuwa mdogo na asiye na uzoefu na hakuweza kuwamudu. [8] Sasa
mnasema kwamba mnaweza kuuzuia utawala wa Yahwe wenye nguvu katika mkono
wa uzao wa Daudi. Ninyi ni jeshsi kubwa, na pamoja nanyi kuna ndama wa dhahabu
ambao Yeroboamu alitengeneza kama miungu kwa ajili yenu. [9] Hamkuwafukuza nje
makuhani wa Yahwe, uzao wa Haruni, na Walawi? Hamkujifanyia makuhani katika
namna ya watu wa nchi zingine? Yeyote ajaye kujitakasa mwenyewe na ngo'mbe
dume kijana, na madume ya kondoo anaweza kuwa kuhani wa kile ambacho siyo
miungu. [10] Lakini kwetu, Yahwe ni Mungu wetu, na hatujamsahau. Tuna makuhani,
uzao wa Haruni, wakimtumikia Yahwe, na Walawi, ambao wako kataika kazi yao.
[11] Kila asubuhi na jioni humtolea Yahwe sadaka za kuteketezwa na uvumba mtamu.

Pia hupanga mkate wa uwepo juu ya meza takatifu; pia huweka kinara cha dhahabu
pamoaja na taa zake, ili watoe sadaka kila jioni. sisi huzishika sheria za Yahwe,
Mungu wetu, Lakini ninyi mmemsahau. 12 Ona, Mungu yuko pamoja nasi katika
vichwa vyetu, na makuhani wake wako hapa na tarumbeta kwa ajili ya kutoa sauti
dhidi yenu. Watu wa Israeli, msipigane na Yahwe, Mungu wa babu zenu, kwa
maana hamtafanikiwa." 13 Lakini Yeroboamu akaandaa mavamizi nyuma yao; jeshi
lake lilikuwa mbele ya Yuda, na wavamizi nyuma yao. 14 Yuda walipoanagalia
nyuma, tanzama, mapigano yalikuwa pote mbele na nyuma yao. Wakamlilia Yahwe
kwa sauti, na makuhani wakayapuliza matarumbeta. 15 Kisha wanaume wa Yuda
wakapiga kelele; walipopiga kele, ikawa kwamba Mungu akampiga Yeroboamu na
Israeli wote mbele ya Abiya na Yuda. 16 Watu wa Israeli wakakimbia mbele ya
Yuda, na akawatia kwenye mkono wa Yuda. 17 Abiya na jeshi lake wakawaua
kwa mauji makuu; 500, 000 watu wanaume waliochaguliwa wa Israeli wakaanguka
wamekufa. 18 Katika namna hii hii, watu wa Israeli wakatiishwa chini wakati huo,
watu wa Yuda wakashinda kwa sababu walimtegemea Yahwe, Mungu wa babu zao.
19 Abiya akamshawishi Yeroboamu; akachukua miji kutoka kwake; Betheli pamoja
na vijiji vyake, Yeshana pamoja na vijiji vyake, na Efroni pamoaaja na vijij vyake.
20 Yeroboamu hakupata naguvu tena katika siku za Abiya; Yahwe akampiga, na akafa.
21 Lakini Abiya akawa na nguvu sana; akachukua wanawake kumi na nne kwa ajili
yake na akawa baba wa wana ishirini na mbili na mabinti kumi na sita. 22 Matendo
ya Abiya yaliyosalia, tabia yake na maneno yake yameeandikwa katika kamusi ya
nabii Ido.

# 14

1 Abiya kalala pamoja na babu zake, na wakamzika kataika maji wa Daudi. Asa,
mwanaye, akawa mfalme katika nafasi yake. Katika siku yake nchi ilikuwa na
miaka kumi. 2 Asa alifanya yaliyomema na sahihi katika macho ya Yahwe Mungu
wake, 3 kwa maana aliziondosha mbali madhabahu za kigeni na sehemu za juu.
Akaziangusha chini nguzo za mawe na kuzikata nguzo za Maashera. 4 Akawaamuru
Yuda kumtafuta Yahwe, Mungu wa babu zao, na kuzishika sheria na amri. 5 Pia
akaziondosha mbali sehemu za juu na madhabahu za kufukiza kutoka miji yote ya
Yuda. Ufalme ulikuwa na pumziko chini yake. 6 Akajenga miji ya ngome katika Yuda,
kwa maana nchi ilikuwa tulivu, na hakuwa na vita katika miaka hiyo, kwa sababu
Yahwe alikuwa amempa amani. 7 Kwa maana Asa aliwaambia Yuda, "Tuijenge miji
hii na kuizungushia kuta, na minara, mageti, na makomeo; nchi bado yetu kwa
sababu tumemtafuta Yahwe Mungu wetu. Tumemtafuta yeye, na ametupa amani
katika kila upande." Kwa hiyo walijenga na wakafanikiwa. 8 Asa alikuwa na jeshi
ambalo lilibeba ngao na mikuki; kutoka Yuda alikuwa na wanaume 300, 000, na
kutoka Benyamini, wanaume 280, 000 waliobeba ngao na kuvuta pinde. 9 Zera
Mwethiopia akaja juu yao na jeshi la wanajeshi milioni moja na magari mia tatu;
akaja Maresha. 10 Kisha Asa akatoka nje kukutana naye, na wakapanga mistari ya vita
ya mapigano katika bonde la Sefatha huko Maresha. 11 Asa kamlilia Yahwe, Mungu
wake,, na akasema, "Yahwe, hakuna aliye kama wewe lakini ni wewe wa kumsaidia
mtu asiye na nguvu anapokutana na mengi. Tusaidie, Yahwe, Mungu wetu, kwa
maana tunakutegemea wewe, na katika jina lako tumekuja kupambana na idadi hii
kubwa ya adui. Yahwe, wewe ni Mungu wetu; usimuache mtu akushinde." 12 Kwa
hiyo Yahwe akawapiga Waethiopia mbele za ASa na Yuda; Waethiopia wakakimbia.
13 Asa pamoja na wanajeshi waliokuwa pamoja naye wakawafukuza hadi Gerari.
Kwa hiyo Waethiopia wengi wakajeruhiwa kiasi kwamba hawakuweza kupona, kwa
maana waliangamizwa kabisa mbele za Yahwe na jeshi lake. Jeshsi likachukua

mateka wengi sana. 14 Jeshi likaviangamiza vijiji vyote jirani na Garari, kwa kuwa
hofu ya Yahwe ilikuwa imekuja juu ya wakaaji. Jeshi likateka vijiji vyote, na
vilikuwa na hazina nyingi sana ndani yake. 15 Jeshi pia likaipiga hema ya makazi
yawachungaji; wakabeba kondoo kwa wingi, ngamia vile vile, na kisha wakarudi
Yerusalemu.

# 15

1 Roho ya Mungu ikaja juu ya Azaria mwana wa Odedi. 2 Akaenda nje kukutana
na Asa na akamwambia, "Nisikilize, Asa, na Yuda wote na Benyamini: Yahwe yuko
pamoja nanyi, pale mnapokuwa naye. Kama mtamtafuta, mtampata; lakini kama
mtamsahau, atawasahau ninyi. 3 Sasa kwa muda mrefu, Israeli hawakuwa na Mungu
wa kweli, bila kuhani wa kufundisha, na bila sheria. 4 Lakini katika dhiki yao
wakamrudia Yahwe, Mungu wa Israeli, na wakamtafuta, wakamta. 5 Katika nyakati
hizo hapakuwa na amani kwake aliyesafiri kwend mbali, wala kwake aliyesafiri
kuja hapa; badala yake shsida kubwa zilikuwa juu ya wenyeji wote wa wanchi.
6 Waligawanyika vikundi vikundi, taifa dhidi ya taifa, na mji dhidi ya mji, kwa
maana Mungu aliwapa shsida za kila aina ya kila mateso. 7 Lakini muwe hodari,
na msiuache mkono wenu kuwa dhaifu, kwa maana kazi yen itapewa thawabu."
8 Asa aliposikia maneno haya, unabii wa odedi nabii, akajipa ujasiri na kuviondosha
mbali vitu vya kuchukiza kutoka nchi yote ya Yuda na Benyamini, na kutoka miji
yote aliyokuwa ameiteka kuanzia kilima cha nchi ya Efraimu, na akaijenga tena
madhabahu ya Yahwe, ambayo ilikuwa mbele ya ukumbi wa nyumba ya Yahwe.
9 Akawakusanya Yuda wote na Benyamini, na wae waliokaa pamoja nao—watu
wa kutoka Efraimu na Manase, na kutoka Simeoni. Kwa maana walikuja kwake
katika hesabu kubwa kutoka Israeli, walipoona kwamba Yahwe Mungu wake alikuwa
pamoja naye. 10 Kwa hiyo wakakusanyika katika Yerusalemu katika mwezzi wa tatu,
katika mwaka wa kumi na tano wa utawala wa Asa. 11 Katika siku hiyo walimtolea
Yahwe dhabihu baadhi ya nyara ambazo walikuwa wameleta; ng'mbe wa kulima
mia saba na kondoo na mbuzi elfu saba. 12 Wakaingia kataika agano kwa ajili ya
kumtafuta Yahwe, Mungu wa babau zao, kwa moyo wao wote na roho yao yote.
13 Wakakubaliana kwamba yeyote atakepuuzia kumtafuta Yahwe, Mungu wa Israeli,
atapaswa kuuawa, iwe mdogo ama mkubwa, iwe mwanaume ama mwanamke.
14 Wakaapa kwa Yahwe kwa sauti kubwa, kwa kelele, na kwa sauti za tarumbeta na
baragumu. 15 Yuda wote wakakifurahia kile kiaapo. kwa maana walikuwa wameapa
kwa moyo wao wote, na walimtafuta Mungu kwa nia yao yote, na walimuona. Yahwe
akawapa amani pande zote. 16 Pia akamwondoa Maaka, asiwe malikia, kwa sababu
alikuwa amefanya sanamu ya kuchukiza ya Maashera. Asa akaivunja vunja sanamu
ya kuchukiza, akaiweka kwenye mavumbi akaichoma moto huko kijitoni Kidroni.
17 Lakini sehemu za juu hazikuwa zimeondolewa nje ya Israeli. Vile vile, Moyo wa
Asa ulijitoa kikamilifu siku zake zote. 18 Akaleta kwenye nyumba ya Mungu vitu
vya baba yake na vitu vyake mwenyewe vilivyokuwa vya Yahwe: vitu vya fedha na
dhahabu. 19 Hapakuwa na vita zaidi hadi miaka thelathini na mitano ya utawala wa
Asa.

# 16

1 Katika mwaka wa thelathini na sita wa utawala wa Asa, Baasha, mfalme wa Israeli,
akatenda kwa ukatili dhidi ya Yuda na akaujenga Rama, ili kwamba asimruhusu
mtu yeyote kutoka wala kuingia katika nchi ya Asa, mfalme wa Yuda.. 2 Kisha
Asa akaitoa fedha na dhahabu nje ya vyumba vya kuhifadhia katika nyumba ya
Yahwe na nje ya nyumba ya mfalme, na akaituma kwa Ben Hadadi mfalme wa
Aramu, ambaye aliishi Dameski. Akasema, pawe na agano kati yako na mimi, kama

palivyokuwa na agano kati ya baba yangu na baba yako. Angalia, nimekutumia
fedha na dhahabu. 3 Livunje agano lako na Baasha, mfalme wa Israeli, ili kwamba
aniache." 4 Ben Hadadi akamsikiliza mfalme Asa na kutuma maakida wa majeshsi
dhidi ya miji ya Israeli. Wakavamia Iyoni, Dani, Abelimaimu, na miji yoye ya
kuhifadhia ya Naftali. 5 Ikawa kwamba Baasha aliposikia hili, akaacha kuujenga
Rama, na akaistisha kazi yake. 6 Kisha Asa mfalme akawachukua Yuda wote pamoja
naye. Wakayabeba mawe na mbao za Rama ambazo Baasha alikuwa anajengea ule
mji. Kisha Mfalme Asa alitumia vifaa hivyo vya ujenzi kwa ajili ya kuijenga Gaba
na Mispa. 7 Wakati huo Hanani mwonaji akaenda kwa Asa, mfalme wa Yuda, na
akamwambia, "Kwa sababu umemtegemea mfalme wa Aramu, na hukumtegemea
Yahwe Mungu wako, jeshi la mfalme wa Aramu limetoroka nje ya mikono yako.
8 Waethiopia na Walubi hawakuwa jesi kubwa, wenye magari mengi na wapanda
farasi wengi? Na bado, kwa sababau ulimtegemea Yahwe, alikupa ushindi juu yao.
9 Kwa maana macho ya Yahwe hukimbia kila mahali katika dunia yote, ili kwamba
ajioneshe mwenyewe shujaa kwa niaba ya wale amabao mioyo yao ni mikamilifu
kumwelekea yeye. Lakini umetenda kipumbavu katika jambo hili. Kwa maana tangu
sasa na kuendelea, utakuwa na vita." Kisha Asa akamkasirikia mwonaji, akamuweka
gerezani, kwa maana alikuwa na hasira naye juu ya jambao 10 hili. Wakati huo
huo, aliwagandamiza baadhi ya watu 11 Tazma, matendo ya Asa, kutoka mwanzo
hadi mwisho, tazama, yameandikwa katika kitabu cha wafalme wa Yuda na Israeli.
12 Katika mwaka wa thelathini na tisa wa utawala wake, Asa alipata ugnjwa kwenye
miguu yake; ugonjwa wake ulikuwa mkali sana. Hata hivyo, hakutafuta msaada
kutoka kwa Yahwe, lakini kutoka kwa waganga tu. 13 Asa akalala pamoja na babu
zake; alikufa katika mwaka wa arobaiani na moja wa utawala wake. Wakamzika
katika kaburi lake, ambalo alilichimba mwenyewe katika mji wa Daudi. 14 Walimlaza
juu ya kitanda kilichokuwa kimewekewa manukato na aina mbali mbali ya dawa
zilizotayarishwa na wale mafundi wa manukato. KIsha wakatengeneza moto kwa
heshima yake.

# 17

1 Yehoshafati mwana wa Asa akawa mfalme katika nafasi yake. Yehoshafati
akajiimarisha dhidi ya Israeli. 2 Akaweka majeshi katika miji yote Yuda yenye
ngome, na akaweka magereza katika nchi ya Yuda na katika miji ya Efraimu, ambayo
Asa baba yake alikuwa ameiteka. 3 Yahwe alikuwa pamoja na Yehoshafati kwa
sababu alitembea katika njia za kwanza za baba yake Daudi, na hakuwatafuta
Mabaali. (Baadhi ya mandiko ya kale hayana "Daudi", na baadhi ya matoleo
ya kisasa yameacha hili jina "Daudi). 4 Badala yake, alimtegemea Mungu wa
baba yake, na alitembea katika amri zake, siyo katika tabia ya Israeli. 5 Kwa
hiyo Yahwe akaimarisha sheria katika mkono wake; Yuda wote wakaleta kodi
kwa Yehoshafati. Alikuwa na utajiri na heshima kubwa. 6 Moyo wake ulikuwa
umejikita katika njia za Yahwe. Pia aliziondoa sehemu za juu na Maashera mbali na
Yuda. 7 Katika mwaka wa tatu wa utawala wake aliwatuma wakuu wake Ben-haili,
Obadia, Zekaria, Nethania, na Mikaya, ili wafundishe katika miji ya Yuda. 8 Pamoja
nao walikuwepo Walawi: Shemaya, Nethanieli, Zebadia, Asaheli, Shemiramothi,
Yehonathani, Adoniya, Tobia, na Tob-adonia, pamoja nao walikuwepo makuhani
Elishama na Yehoramu. 9 Walifundisha katika Yuda, wakiwa na kitabau cha sheria
ya Yahwe. Wakaenda karibu miji yote ya Yuda na kufundisha miongoni mwa watu.
10 Hofu ya Yahwe ikashuka juu ya falme zote za nchi, zilizouzunguka Yuda, kwa hiyo
hazikufanya vita dhidi ya Yehoshafati. 11 Baadhi ya Wafilisti wakamletea Yehoshafati
zawadi, fedha kama kodi. Waarabu pia wakamletea makundi, 7, 700 kondoo waume,

na mbuzi 7, 770. [12] Yehoshafati akawa na nguvu sana. [13] Akajenga ngome na miji ya
maghala katika Yuda. Alikuwa na kazi nyingi katika miji ya Yuda, na wanajeshsi—
imara, wanaume hodari—katika Yerusalemu. [14] Hapa ni rodha yao, wamepangwa
kwa majina ya nyumba za baba zo: Kutoka Yuda, maakida wa maelfu; Adna yule
jemedari, na pamoja naye wanaume wa kwenda vitani 300, 000; [15] akifuatiwa na
Yehonani jemedari, na pamoja naye wanaume 280, 00; [16] akifuatiwa na Amasia
mwana wa Zikri, ambaye kwa hiari alijitoa kumtumikia Yahwe; na pamoja naye
wanaume wa kwenda vitani 200, 000. [17] Kutoka Benyamini: Eliada mtu jasiri, na
pamoja naye watu 200, 000 waliovaa upinde na ngao; [18] akifutiwa na Yehozabadi, na
pamoja naye askari 180, 000 waliotayari kwa vita. [19] Hawa walikuwa ni wale ambao
walimtumikia mfalme, miongoni mwao wale ambao mfalme aliwaweka katika miji
ya ngome katika Yuda yote.

# 18

[1] Sasa Yehoshafati alikauwa na utajiri mwingi na heshima kubwa; alifanya undugu
na Ahabu mmoja wa watu wa familia yake akamuo binti yake. [2] Baada ya miaka
kadhaa, akashsuka chini kwa Ahabu huko Samaria. Ahabu akachinja kondoo
na ngo'mbe wengi kwa ajili ya yake na watu waliokuwa pamoja naye. Ahabu
pia akamshawishi kuivamia Ramothi-gileadi pamoja naye. [3] Ahabu, mfalme wa
Israeli, akamwambia Yehoshafati, mfalme wa Yuda, “Utakwenda Ramothi-gileadi
pamoja nami?” Yehoshafati akamjibu, “Mimi ni kama wewe, na watu wangu ni
kama watu wako; tutakuwa pamoja nawe katika vita.” [4] Yehoshafati akamwambia
mfalme wa Israeli, Tafadhali litafute neno la Yahwe kwanza kwa ajili ya jibu
lako” [5] Kisha mfale wa Israeli akawakusanya manabii pamoja, wanauame mia nne,
na akasema akwao, Tutaenda vitani Ramothi-gileadi, au nisiende?” Wakasema,
“Vamia, kwa maana Mungu ataitia mkononi mwa mfalme.” [6] Lakini Yehoshafati
akasema, “Hakuna nabii mwingine hapa wa Yahwe ambaye kwake tunapaswa
kutafuta ushauri?” [7] Mfale wa Israeli akamwambia Yehoshafati, Bado kuna mtu
mmoja amabaye kwake lazima tuutafute ushauri wa Yahwe, Mikaya mwana wa
Imla, lakini namchukia kwa sababu yeye huwa hatabiri mema kamwe kuhusu mimi,
bali kila mara maovu,” Lakini Yehoshafati akasema, “ Mfalme hapaswi kusema
hivyo.” [8] Kisha mfalme wa Israeli akamwita akida na kusema, Haraka mlete Mikaya
mwana wa Imla.” [9] Sasa Ahabu mfalme wa Israeli na Yehoshafati mfalme wa
Yuda walikuwa wamekaa kila mmoja katika kiti cha enzi, wamevalia kanzu zao,
katika sehemu ya uwazi katika maingilia ya lango la Samaria, na manabii wote
walikuwa wakitabairi mbele zao. [10] Zedekia mwana wa Kenaani akajitengenezea
pembe za chuma na kusema, Yahwe anasema hivi: Kwa kutumia hizi pembe
mtawasukuma Waaramu hadi waangamie.” [11] Manabii wote wakatabiri kitu kile
kile, wakisema, “Vamia Raamothi-gleadi na shinda. kwa maana Yahwe ameutia
kwenye mkono wa mfalme.” [12] Mjumbe aliyeenda kumuita Mikaya akasema kwake,
akisema, “Sasa angalia, maneno ya manabii yanatangaza mambo mema kwa ajili
ya mfalme kwa kinywa kimoja. Tafadhali maneno yako yawe kama maneno ya
mmoja wao na sema mambo mema.” [13] Mikaya akajibu, “Kama Yahwe aishivyo,
mimi nitasema kile mbacho Mungu anasema.” [14] Alipokuja kwa mfalme, mfamle
akamwambaia, “Mikaya, tutaenda Ramothi -gileadi kwa ajili ya vita, au la?” Mikaya
akamjibu, “Vamia na utashinda! kwa maana utakuwa ushinda mkuu.” [15] Kisha
mfalme akasema kwake, “Ni mara ngapi ninapaswa kukutaka kuapa kutoniambia
kitu chochote sispokuwa kweli katika jina la Yahwe? [16] Kwa hiyo Mikaya akasema,
“Niliwaoana Israeli wametawanyika ktika mlima, kama kondoo wasio na mchungaji,
na Yahwe akasema, hawa hawana mchungaji. Ebu kila mtu arudi nyumbani kwake

kwa amani.” 17 Kwa hiyo mfalme wa Israeli akamwambia Yehoshafati, “Sikukuambia
kwamba asingeweza kutabiri mema juu yangu, bali majanga tu? 18 Kisha Mikaya
akasema, “Kwa hiyo ninyi nyote mnapashwa kulisikia neno la Yahwe: Nilimuon
Yahwe amekaa juu ya kiti chake cha enzi, na majeshi yote ya mbinguni yalikauwa
yamekaa mkono wake wa kulia na mkono wake wa kushoto. 19 Yahwe akasema, Ni
nani atakayemrubuni Ahabu, mfalme wa Israeli, ili kwamba aende na kuanguka huko
Ramothi-gileadi?' Mmoja alisema hivi na mwingine hivi. 20 Kisha roho ikaja moja kwa
maja na kusimama mbele ya Yahwe na kusema, 'Nitamrubuni.' Yahwe akamwambia,
'Kivipi?' 21 Roho ikajibu, “nitatoka nje na nitakuwa roho ya uongo katika vinywa
vya manabii wake wote.' Yahwe akajibu, 'utamrubuni, na pia utafanikiwa. nenda
sasa na fanya hivyo.' 22 Sasa ona, Yahwe ameweka roho ya uongo katika midomo
ya manabii wako hawa, na Yahwe ametangaza majanga kwa ajili yako.” 23 Kisha
Zedekia mwana wa Kenaana, akaja, akampiga kofi mika juu ya shavu, na kusema,
“Kwa njia gani Roho wa Yahwe alitoka kwangu ili aseme nawe?” 24 Mika akasema,
Angalia, utalijua hilo katika siku hiyo, mtakapokimbia katika baadhi ya vyumba
vya ndani kwa ajili ya kujificha.” 25 Mfalme wa Israeli akasema kwa baadhi ya
watumishi, “ Enyi watu mkamateni Mikaya na mmpeleke hadi Amoni, mkuu wa
mji na, na kwa Yoashi, mwanangu. 26 Nanyi mtamwambia, 'Mfalme anasema:
Mweke gerezanai huyu mtu na umlishe kwa mkate kiogo tu na maji kidogo tu,
mpaka nitakaporudi salama.” 27 Kisha Mikaya akasema, “Kama utarudi salama,
Yahwe hajasema nami.”Kisha akaongeza, “Sikiliza haya, enyi watu wote.” 28 Kwa
hiyo Ahabu, mfalme wa Israeli, na Yehoshafati, mfalme wa Yuda, wakaenda juu
ya Ramothi-giledi. 29 Mfalme wa Israeli akamwamabia Yehoshafati, “Nitajibadilisha
mwenyewe na kwenda vitani, lakini wewe vaa mavazi yako ya kifalme.” Kwa hiyo
mfalame wa Israeli akajibalisha, na wakaenda vitani. 30 Sasa mfalme wa Aramu
alikuwa amewaamuru maakida wa magari yake, akisema, Msiwavamie wanajeshsi
wasio wa muhimu wala wanajeshsi muhimu. Badala yake, mvamieni mfalme wa
Israeli pekee,” 31 Ikawa kwamba maakida wa magari walipomuona Yehoshafati
wakasema, “Yule ni mfalme wa Israeli.” Wakageka kumzunguka wamvamie, lakini
Yehoshafati akalia, na Yahwe akamsaidia. Mungu akawageza nyuma kutoka kwake.
32 Ikawa kwamba maakida wa magari walipoona ya kuwa hakuwa mfalme wa Israeli,
wakarudi nyuma wasimfukuze. 33 Lakini mtu mmoja akauvuta upinde wake kwa
kubahatisha na kumpiga mfalme wa Israeli kati kati ya maungio ya mavazi yake.
Kisha Ahabu akamwambia dereva wa gari lake, “Geuza nyuma na nitoe nje ya
mapigano, kwa maana nimejeruhiwa vibaya sana.” 34 Mapigano yakazidi kuwa
makali siku hiyo, na mfalme wa israeli akashikiliwa katika gari lake kuwaelekea
Waaramu hadi jioni. Muda jua lilipokaria kwenda chini, akafa.

# 19

1 Yehoshafati mfalme wa Yuda akarudi salama nyumbani kwake Yerusalemu.
2 Kisha Yehu mwana wa Hanani, mwonaji, akatoka kukutana naye na akasema kwa
mfalme Yehoshafati, “Unapaswa kuwa unawasaidia waovu? Unapaswa kuwapenda
wanaomchukia Yahwe? Kwa ajili ya tendo hili, ghadhabu toka kwa Yahwe iko
juu yako. 3 Aidha, kuna baadhi ya mema ya kuonekana ndani yako, kwamba
umeziondosha Maashera nje ya nchi, na umeukaza moyo wako kumtafuta Mungu.”
4 Yehoshafati akaishi katika Yerusalemu; na akaenda nje tena miongoni mwa watu
wa Beer- sheba hadi nchi ya kilima ya Efraimu na akawarudisha kwa Yahwe, Mungu
wa baba zao. 5 Akaweka waamuzi katika nchi katika miji yote ya Yuda yenye
angome, mji kwa mji. 6 Akawaambia waamuzi, “Zingatieni mnachopaswa kufanya,
kwa sababu hamuamui kwa ajili ya mwanadamu, bali kwa ajili ya Yahwe; yuko

pamoja nanyi katika kazi ya kuamua, 7 Basi sas iacheni hofu ya Mungu iwe juu yenu.
Iweni waangaliafu mnapoamua, kwa maana hakuna uovu wa Yahwe Mungu wetu,
wala hakuna upendeleo wala hongo." 8 Vile vile, katika Yerusalemu Yehoshafati
akateua baadhi ya Walawi na makuhani, na baahdhi ya viongozi wa nyumba za
mababu wa Israeli, kwa ajili ya kufanya hukumu kwa ajili ya Yahwe, na kwa ajili ya
migogoro. Wakaishi katika Yerusalemu. 9 Akawaelekeza, akisema, "Lazima mtumike
kwa heshima kwa ajaili ya Yahwe, kwa uaminifu, na na kwa moyo wenu wote. 10 Kila
mgogoro wowote utakapokuja kwenu kutoka kwa ndugu zenu wanaoishi katika miji
yao, iwe inahusu mauji, iwe inhusu torati na amri, lazim muwaonye, ili kwamba
wasiwe na hatia mbele za Yahwe, la sivyo ghadhabu itakuja juu yenu na juu ya
ndugu zenu. Mnapaswa kufanya hivyo na hamtakuwa na hatia 11 Ona, Amaria
kuhani mkuu yuko juu yenu katika mambo yote ya Yahwe. Zebadia mwana wa
Ishmaeli, kiongozi wa nyumba ya Yuda, ni kiongozi katika yote katika mambo yote
ya mfalme. Pia, Walawi watakuwa wasimamizi wakiwatumikia ninyi. Muwe hodari
na tiini maelekezo yenu, na Yahwe awe moja nao walio wema."

# 20

1 Ikawa baada ya hayo, kwamba watu wa Moabu na Amoni, na pamoja na
baadhi ya Wameuni wakaja juu ya Yehoshafati ili kupigana vita. (Mandishi, "baadhi
ya Wameuni" yanatoa masahihisho kwa ajili ya maandishi ya Kiebrania, ambayo
yanasomeka, "baadhi ya Waamoni". Inadhaniwa kwamba "Wameuni" ndilo neno la
asili, na wenye kunukuu walilibadili kuwa "baadhi ya Waamoni". Lakaini jina hili la
mwisho halileti maana, kwa sababu Waamoni tayari wamekwisha tajwa katika mstri
huu. Vile vile, matoleo tofauti tofauti yanajihusha na tatizo hili katika namna mabli
mbali) 2 Kisha baadhi ya watu wakaja wakamwambia Yehoshafati, wakisema, "Umati
mkubwa wanakuja juu yako ng'ambo ya Bahari iliyokufa, kutoka Edomu. Ona, wako
Hason- tamari", ambayo ndiyo En-gedi. (Badala ya "Edomu" baadhi ya matoleo ya
zamani na ya kisasa yanasomeka, "Aramu." 3 Yehoshafati akaogopa na akajipanga
kumtafuta Yahwe. Akatangaza haraka katika Yuda yote. 4 Yuda wakakakusanyika
pamoja kwa ajili ya kumtafuta Yahwe; wakaja kutoka miji yote ya Yuda kwa
ajili ya kumtafauta Yahwe. 5 Yehoshafati akasimama katika kusanyiko la Yuda na
Yerusalemu, kwenye nyumba ya Yahwe, mbele ya kibaraza kipya. 6 Akasema, "Yahwe,
Mungu wa babau zetu, hauko mbinguni? Wewe siyo mtawala juu ya falame zote za
mataiafa? Nguvu na uweza viko mkononi mwako, kwa hiyao hakuna anayeweza
akukupinga wewe. 7 Munagu wetu, Hukuwafuaakuja nje wakaaji wa nchi hii mbe
ya watau watau wakop Israeli, na kuitoa milele kwa ajili ya uzaoa wa Abrahamu?
8 Wakaishi ndani yake na kujenga sehemu takatifu kwa ajili ya jina lako, wakisema,
9 'Ikiwa janga litakuja juu yetu —upanga, hukumu, au ugonjwa, au njaa—tutasimama
mbele ya nyumba hii, na mbele zako (kwa maana jina lako limo ndani ya nyumba
hii), na tutakulilia wewe katika mateso yetu, na utatusikia na kutuokoa.' (Badala ya
"hukumu" baadhi ya maandiko ya zamani yanasema "mafuriko"). 10 Tazama sasa,
hapa kuna watu wa Amoni, Moabu, na wa Mlima Seiri ambao hukuwaacha Israeli
wawapige waalipotoka nchi ya Misri; badala yake, Israeli waliwageukia mbali na
hawakuwaangamiza. 11 Ona jinsi wanavyotuzawadia; wanakuja kutotoa nje ya nchi
yako mbayo umetupa kuirithi. 12 Mungu wetu, hutawahukumu? Kwa maana hatuna
nguvu dhidi ya hili jeshi kubwa ambalo linakuja juu yetu. hatujui cha kufanya,
lakini macho yetu yako kwako. 13 Yuda wote wakasimama mbele ya Yahwe, pamoja
na wadogo wao, wake, na watoto. 14 Kisha kati kati ya kusanyiko, roho ya Yahwe
ikaja juu ya Yahazieli, mwana wa Zekaria, mwana wa Benaya, mwana wa Yeieli,
mwana wa Matania, mwana, Mlawi, mmoja wa wana wa Asafu. 15 Yahazieli akasema,

“Sikilizeni, Yuda wote na ninyi wakaaji wa Yerusalemu, na Mfalme Yehoshafati. Hivi
ndivyo Yahwe asemavyao kwenu, 'Msiogope: msivunjike moyo kwa sababu ya hili
jeshsi kubwa, kwa maana vita siyo yenu, bali ni ya Mungu. 16 Lazima muende
chini juu ya yao kesho, Ona, wanakuja wakipanda kupia njia ya Sisi. Mtawakuta
mwishono mwa bondo, mbele ya jangwa la Yerueli. 17 Hamtahitaji kupigana katika
vita hii. Simameni katika nafasi zenu, simameni wima, na muone wokovu wa
Yahwe pamoja nanyi, Yuda na Yerusalemu. Msiogope wala kukata tamaa. Tokeni
nje juu yao kesho, kwa maana yuko pamoja nanyi.” 18 Yehoshafati akainamisha
kichwa chake pamaoja na uso wake chini. Yuda wote na wakaaji wa Yerusalemu
wakaanguka chini mbele za Yahwe, wakimwabudu yeye. 19 Walawi, wale wa uzao
wa Wakohathi na wa uzao wa Wakorahi, wakasimama juu kumsifu Yahwe, Mungu
wa Israeli, kwa sauti kubwa sana. 20 Asubuhi mapema wakasimama na kwenda
nje kwenye bonde la Tekoa. Walipokuwa wakienda nje, Yehoshafati akasimama
na kusema, “Nisikilizeni, Yuda, na nnyi wakaaji wa Yerusalemu! Aminini katika
Yahwe Mungu wenu, na mtasaidiwa. Aminini katika manabii zake, na mtafanikiwa.
21 Alipokuwa ameshauriana na watu, akawachagaua wale ambao wangemwimbia
Yahwe na kumpa sifa kwa ajili ya utukufu wake mtakatifu, walipokuwa wakienda
wakilitangulia jeshi, na kusema, “Mshukuruni Yahwe, kwa maana uaminifu wa
aganao lake unadumu milele.” 22 Walipoanza kuimba na kusifu, Yahwe akapanga
wanaume katika mavamizi juu ya watu wa Amoni, Moabu, na wa Mlima Seiri, ambao
walikuwa wanakauja dhidi ya Yuda. Walishindwa. 23 Kwa maana watu wa Aamoni
na Moabu walisimama kupigana na wakaaji wa Mlima Seiri, ili kuwaua kabisa
na kuwangamiza. Waliapokuwa wamemaliza kuwaangamiza wakaaji wa Mlima
Seiri, wote wakasaidiana kuangamizana kila mmoja. 24 Yuda walipokuwa katika
sehemu hiyo wakiangalia jangwani, waliangalia nje juu ya jeshi. Tazama, walikuwa
wamekufa, wameanguka chini; hakuna aliyekuwa amepona. 25 Yehoshafati na watu
wake walipokuja kuchukua nyara kutoka kwa hao watu, walikuta miongoni mwao
bidhaa nyingi, nguo, na johari za thamani, ambazo walizichukua kwa ajili yao
wenyewe, nyingi kuliko uwezo wao wa kubeba. Iliwachukua siku tatu kusomba nyara
hizo, zilikuwa nyingi sana. (Badala ya “miongoni mwao”, baadhi ya maandishi ya
zamani na ya kisasa yanasema, “ng'ombe.” badala ya “nguo” baadhi ya maandiko ya
kale na ya kisasa yanasema, “miili iliyokufa”). 26 Katika siku ya nne wakakusanyika
katika bonde la Baraka, Huko wakamsifu Yaahwe, kwa hiyo jina la sehemu hiyo hata
leo ni “Bonde la Baraka”. 27 Kisha, wakarudi, kila mtu wa Yuda na Yerusalemu, na
Yehoshafati katika uongozi wao, kwenda tena Yerusalemu kwa furaha, kwa maana
Yahwe alikuwa amewafanya wafurahie juu ya adui zao. 28 Wakaja Yerusalemu na
kwenye nyumba ya Yahwe kwa vinanda, vinubi na matarumbeta. 29 Hofu ya Yahwe
ikawa juu ya falme zote za mataifa waliposikia kwamba Yahwe amepigana dhidi ya
adui wa Israeli. 30 Kwa hiyo ufaleme wa Yehoshafati ulikuwa mtivu, kwa maana
Mungu wake alimpa amani kuzungunga pande zake zote. 31 Yehoshafati akatawala
juu ya Yuda: Alikuwa na umri wa miaka thelathini na mitano alipoanza kutawala.
Jina la mama yke aliitwa Azubahi, binti wa Shilhi. 32 Akatembea katika njia za Asa,
baba yake; hakugeka popote kuziacha; akafanya yaliyo mema katika macaho ya
Yahwe. 33 Vile vile, sehemu za juu hazikuwa zimeondoshwa mbali. Watu walikuwa
bado hawajaelekeza mioyo yao kwa Mungu wa babu zao. 34 Kwa mambo mengine
kuhusu Yehoshafati, mwanzo na mwisho, tazama, yameandikwa katika historia ya
kitabu cha wafalme wa Israeli. 35 Baada ya hayo, Yehoshafati, mfalme wa Yuda,
akapatana na Ahazia, mfalme wa Israeli, ambaye alitenda uovu mwingi. 36 Akapatana
naye kujenga meli za kwenda Tarshishi; Wakazijenga meli hizo huko Esion-geberi.
37 Kisha Eliezeli, mwana wa Dadavahu wa Maresha, akatoa unabii juu ya Yehoshafati;

akasema, “kwa sababu umepatana na Ahazia, Yahwe ameiharibu miradi yako.” Meli zilivunjika ili kwamba zisiweze kusafiri.

# 21

[1] Yehoshafati akalala pamoja na babu zake na akizikwa pamoaja nao katika mji wa
Daudi; [2] Yehoramu, mwanaye, akawa mfalme katika nafasi yake. Yehoramu alikuwa
na ndugu, wana wa Yehoshafati: Azaria, Yerieli, Zekaria, Azaria, Mikaeli, na Shefatia.
Wote hawa walikuwa wana wa Yehoshafati, mfalme wa Israeli. [3] Baba yao alikuwa
amewapa zawadi kubwa ya fedha, dhahabu, na vitu vingine vya thamani, na miji
yenye ngome katika Yuda, lakini kiti cha enzi alimpa Yehoramu, kwa sababu alikuwa
mzaliwa wake wa kwanza. [4] Sasa Yehoramu alipokuwa ameinuka katika ufalme wa
baba yake na kujiimarisha mwenyewe kama mfalme, akawaua ndugu zake wote kwa
upanga, na pia viongizi wengine mbali mbali wa Israeli. [5] Yehoramu alikuwa na umri
wa mika thelathini na mbili alipoanza kutawala, na akatawala kwa miaka minane
katika Yerusalemu. [6] Akatembea katika njia za wafalme wa Israeli, kama nyumba ya
Ahabu ilivyokuwa ikifanya, kwa maana alikuwa na binti Ahabu kama mke wake,
na akafanya yaliyo maovu katika macho ya Yahwe. [7] Vile vile, Yahwe hakutaka
kuiangamiza nyumba ya Daudi, kwa sababu ya agano ambalo alikuwa amefanya na
Daudi; alikuwa ameahidi kwamba siku zote angetoa uzima kwa ajili yake na kwa ajili
ya vizazi vyake. [8] Katika siku za Yehoramu, Edomu wakaasi wasiwe chini ya Yuda,
na wakajisimamishia mfalme juu yao. [9] Kisha Yeroboamu akavuka ng'ambo pamoja
na maakida na magari yake yote. Ilikuwa usiku aliposimama na kupigana dhidi ya
Waedomu ambao walikuwa wamemzunguka na maakida wa magari yake. [10] Kwa
hiyo Edomu iliasi kutoka kuwa chini ya Yuda mpaka leo. Libna pia aliasi wakati ule
ule wasiwe chini yake. Kwa sababu Yehoramu alikuwa amemsahau Yahwe, Mungu
wa babu zake. [11] Zaidi ya hayo, Yehoramu pia alikuwa amezijenga sehemu zake za
juu katika milma ya Yuda na akawafanya wakaaji wa Yuda kuishi kama makahaba,
na akawaongoza Yuda katika upotevu. [12] Barua kutoka kwa nabii Eliya ikaja kwa
Yerohamu. Ilisema, “Hivi ndivyo Yahwe, Mungu wa Daudi, babu yako, anasema:
Kwa sababu hujatembea katika njia za Yehoshafafati, baba yako, wala katika njia
za Asa, mfalme wa Yuda, [13] bali umetembea katika njia za wafalme wa Israeli,
na umewafanya Yuda na wakaaji wa Yerusalemu kuenenda kama kahaba, kama
nyumba ya Ahabu walivyofanya—na kwa sababu pia umewaua ndugu zako katika
familia ya baba yako kwa upanga, watu waliokuwa bora kuliko wewe mwenyewe—
[14] ona, Yahwe atawapiga watu wako na pigo kubwa, watoto wako, wake zako, na
mali zako zote. [15] Wewe mwenyewe utakuwa na ugonjwa mwingi kwa sababu
ya ugonjwa kataika katika utumbo wako, mpaka utumbo wako uanguke nje kwa
sababu ya ugonjwa, siku baada ya siku. [16] Yahwe akaichochea roho ya Wafilisiti
dhidi ya Yuda na ya Waarabu waliokuwa karibu na Waethipia. [17] Wakaivamia Yuda,
wakavamia katika nyumba ya mfalme. Pia wakawachukua wanaye na wake zake.
Hakuna mwana aliyebakizwa kwa ajili yake ispokuwa, Yehoshafati, mwanaye mdogo.
[18] Baada ya haya yote, Yahwe akampiga katika utumbo wake kwa ugonjwa usiopona.
[19] Ikawa wakati ulipofika, katika mwisho wa miaka miwili, kwamba utumbo wake
ukaaanguka nje kwa sababu ya ugonjwa wake, na kwamba akafa kwa ugonjwa mkali.
Watu wake hawakutengeneza moto kwa ajili ya heshima yake kama walivyokuwa
wamefanyia babu zake. [20] Alikuwa ameanza kutawala alipokuwa na umrai wa miaka
thelatahini na mbaili; akatawala katika Israeli kwa miaka minane, na alikufa bila
kuaombolezwa. Wakamzika katika mji wa Daudi, lakini siyo katika makaburi ya
kifalme.

# 22

[1] Wakaaji wa Yersusalemu wakamfanya Ahazia, mwana mdodgo wa Yehoramu,
mfalme katika nafasi yake, kwa maana kundi la watu ambalo lilikuja na Waarabu
katika ngome lilikuwa limewauwa wanaye wakubwa wote. Kwa hiyo Ahazia mwana
wa Yehoramu, mfalme wa Yuda, akawa mfalme. [2] Ahazia alikuwa na umri wa
mika arobaini na mbili alipoanza kutawala; alitawala kwa mwaka mmoja katika
Yerusalemu. Jina la mama yake aliitwa Athalia; alikuwa binti Omri. [3] Pia Ahazia
alitembea katika njia za nyumba ya Ahabu kwa maana mama yake alikuwa mshauri
katika kufanya mamabo maovu. [4] Ahazia alifanya yaliyokuwa maovu katika macho
ya Yahwe, kama nyumba ya Ahabu walivyokuwa wakifanya, kwa maana walikuwa
washauri wake baada ya kifo cha baba yake, hadi kuangamia kwake. [5] Pia aliufuata
ushauri wao; akaenda pamoja na Yoramu mwana wa Ahabu, mfalme wa Israeli,
kwa ajili ya kupigana dhidi ya Hazaeli, mfalme wa Aramu, huko Ramothi-gileadi.
Waaramu wakamjeruhi Yoramu. [6] Yoramu akaraudi Yezreeli kwa ajili ya kuponywa
majeraha ambayo walipa huko Rama, alipopigana dhidi ya Hazaeli, mfalme wa
Aramu. Kwa hiyo Ahazia mwana wa Yehoramu, mfalme wa Yuda, akaenda chini
Yezreeli ili kumuona Yoramu mwana wa Ahabu, kwa sababu Yoramu alikuwa
amejeruhiwa. [7] Sasa uharibifu wa Ahazia ulikuwa umeletwa na Mungu kupitia
kutembelewa na Yoramu. Alipokuwa amewasiri, alienda pamoja na Yeharamu ili
kumvamia Yehu mwana wa Nimshi, ambaye Yahwe alikuwa amemchagua kwa
ajili ya kuingamiza nyumba ya Ahabu. [8] Ikawa kwamba, Yehu alikuwa akichukua
hukumu ya Mungu juu ya nyumba ya Ahabu, kwamba aliwakuta viongozi wa Yuda
na wana wa ndugu zake Ahazia wakimtumikia Ahazia. Yehu akawauwa. [9] Yehu
akamtafuta Ahazia; Wakamkamata akiwa amejificha katika Samaraia, wakamleta
kwa Yehu, na wakamuuwa. Kisha wakamzika, kwa maana walisema, "Ni mwana wa
Yehoshafati, ambaye alimtafuta Yahwe kwa moyo wake wote." Kwa hiyo nyumba
ya Ahazia haikuwa na nguvu zaidi kwa ajili ya kuutawala ule ufalme. [10] Sasa
Athalia, mama wa Ahazia, akaoana kwamba mwanaye alikuwa amekufa, akaianuka
na kuwauwa watoto wote wa kifalme katika nyumba ya Yehu. [11] Lakini Yehoshaba,
binti wa mfalme, akamchukua Yoashi, mwana wa Ahazia, na akamvutia mbali kutoka
miongoni mwa wana wa mfalme ambao waliuawa. Akamuweka yeye na mlezi wake
katika chumba cha kulala. Kwa hiyo Yehoshaba, binti wa mfalme Yehoramu, mke
wa Yehoiada kuhani (kwa maana alikuwa dada yake Ahazia), akamficha asimuone
Athalia, kwa hiyo Athalia hakumuuwa. [12] Alikuwa pamoja nao, wakiwa wamejificha
katika nyumba ya Mungu kwa miaka sita, Athalia alipotawala juu ya Yuda.

# 23

[1] Katika mwaka wa sa saba, Yehoyada alionesha nguvu zake na akaingia katika
agano na maakida wa mamia, Azaria mwana wa Yerohamu, Ishmaeli mwana wa
Yehohanani, Azaria mwana wa Obedi, Maaseya mwana wa Adaya, na Elishafati
mwana wa Zikri. [2] Wakaenda katika Yuda na kuwakusanya Walawi kutoka miji
yote ya Yuda, vile vile na wakuu wa nyumba za mababu wa Israeli, na wakaja
hadi Yerusalemu. [3] Kusanyiko lote wakafanya aganao na mfalme katika nyumba ya
Mungu. Yehoyada akawaambia, "Ona, mwana wa mfalme atatawala, kama Yahwe
alivyosema kuhusu uzao wa Daudi. [4] Hivi ndivyo mtakavyo fanya: theluthi yenu
makuhani na Walawi ambao huja kuhudumu siku ya Sabato, mtakuwa walinzi
katika milango. [5] Theluthi nyingine mtakuwa katika nyumba ya mfalme, na theluthi
nyingine mtakuwa katika Msingi wa Lango. Watu wote watakuwa katika uwanja
wa nyumba ya Yahwe. [6] Msimruhusu yeyote kuingia kwenye nyumba ya Yahwe,
isipokuwa makuhani na Walawi wanaoatumika. Wao wanaweza kuingia kwa sababu

inawahusu. 7 Lakini watu wengine wote lazima mtii amri ya Yahwe. Walawi lazima
wamzunguke mfalme pande zote, kila mtu na silaha zake mkononi mwake. Yeyote
atakayeingia katika nyumba, atauawa. Kaeni na mfalme aingiapo ndani na atokapo
nje." 8 Kwa hiyo Walawi na Yuda wote walitumika kwa kila njia kama katika namna
ambayo Yehoyada kuhani aliwaamuru. Kila mmoja alichukua watu wake, wale
waliotakiwa kuja ndani kuhudumu katika Sabato, na wale watakaoondoka siku ya
Sabato, kwa maana 9 Yehoyada, kuhani, hakuwa amezuilia mojawapo ya zamu zao.
Kisha Yeliyadaya, kuhani, akaleta kwa maakida mikuki na ngao ndogo na kubwa
zilizokuwa za mfalme Daudi ambazo zilikuwa katika nyumba ya Mungu. 10 Yehoyada
akawaleta wanajeshi wote, kila mtu na mkuki wake katika mkono wake, upande wa
kulia wa hekalu hadi upande wa kushoto wa hekalu, pembeni mwa madhabahu
na hekalu, wakimzunguka mfalme. 11 Kisha wakamleta nje mwana wa mfalme,
wakaiweka taji juu yake, na kumpa agano la sheria. Kisha wakamfanya mfalme,
na Yehoyda na wanaye wakampaka mafuta. Kisha wakasema, "Aishi maisha marefu
mfalme." 12 Athalia aliposikia kele za watu wakikimbia na kumsifu mfalme, akatoka
ili awaone watu katika nyumba ya Yahwe. 13 na akaangalia, na, tazama, mfamle
alikuwa amesimama karibu na nguzo yake katika lango la, kuingilia na maakida
na wapuliza tarumbeta walikuwa karibu na mfame. Watu wote wa nchi walikuwa
wakifurahia na kupuliza tarumbeta na waimbaji walikuwa wakipiga vyombo vya
muziki na kuongoza nyimbo za kusifu. Kisha Athalia akayararua mavazi yake na
kupiga kelele. "Fitina! Fitina!" 14 Kisha Yehoyada, kuhani, akawaleta nje maakida
wa mamia waliokuwa juu ya jeshi na kusema, "Mleteni nje kati ya safu, yeyote
atakayemfuata, auwawe kwa upanga." kwa maana kuhani alikwishasema, "Msimuue
katika nyumba ya Yahwe." 15 Kwa hiyo wakafanya njia kw ajili yake, na akaenda
kwenye nyumba ya mfalme kupita njia ya Lango la Farasi, na huko wakamuuwa.
16 kisha Yehoyada alifanya agano kati yake mwenyewe, watu wote, na mfalme,
kwamba watakuwa watu wa Yahwe. 17 Kwa hiyo watu wote wakaenda kwenye
nyumba ya Baali na kuiangusha chini. wakazivunja vipande vipande madhabahu za
Baali na sanamu zake, na wakamuua Matani, kuhani wa Baali, mbele ya madhabahu
hizo. 18 Yehoyada akateua wakuu kwa ajili ya nyumba ya Yahwe chini ya mkono wa
makuhani, ambao walikuwa Walawi, ambao Daudi alikuwa amewapanga kwenye
nyumba ya Yahwe, ili wamtolee Yahwe sadaka za kuteketezwa, kama ilivyoandikwa
katika sheria ya Musa, pamoja na kushangilia na kuimba, kama alivyotoa maelekezo
Daudi. 19 Yehoyada akaweka walinzi katika malango ya nyumba ya Yahwe, ili
kwamba kwa namna yoyote ile asiingie mtu asiyesafi. 20 Yehoyada akachukua pamoja
naye maakida wa mamia, watu wakubwa, watawala wa watu, na watu wote wa nchi.
Akamleta chini mfalme kutoka kwenye nyumba ya Yahwe; watu wakaja kwenye
nyumba ya mfalme kupitia Lango la juu na kumkalisha mfalme juu ya kiti cha
enzi cha ufalme. (Baadhi ya maandiko ya ya kisasa yanasema, "wakamshusha chini
mfalme") 21 Kwa hiyo watu wote wa nchi wakafurahia, na mji wote ulikuwa kimya.
Kuhusu Asa walikuwa wamemuua kwa upanga.

# 24

1 Yoashi alikuwa na umri wa miaka saba alipoanza kutawala; akatawala kwa mika
arobaini katika Yerusalemu. Jina la mama yake aliitwa Sibia wa Beer-sheba. 2 Yoashi
alifanya yaliyo mema katika macho ya Yahwe siku zote za Yehoyada, yule kuhani.
3 Yehoyada akajichukulia wake wawili kwa ajili yake, na akawa baba wa wana na
mabinti. 4 Ikawa baada ya haya, kwamba Yoashi aliamua kuitengeneza nyumba
ya Yahwe. 5 Akawakusanya pamoja makuhani na Walawi, na kusema kwao, "
Nendeni nje kila mwaka kwenye miji ya Yuda na kukusanya fedha kutoka Israeli yote

kwa ajili ya kuikarabati nyumba ya Mungu wenu. Hakikisheni kwamba mnaanza
haraka." Walawi hawakufanya kitu kwanza. 6 Kwa hiyo mfalme akamuita Yehoyada,
yule kuhani, na kumwambia, "Kwa nini hukuwaagiza Walawi kuleta kutoka Yud
na Yerusalemu kodo iliyoagizwa na Musa mtumishi wa Yahwe na kusanyiko la
Israeli, kwa ajili ya amri za hema ya agano?" 7 Kwa maana wana wa Athalia,
yule mwanamke muovu, walikuwa wameivunja nyumba ya Mungu na kuwapa
Mabaali vitu vyote vitakatifu vya nyumba ya Yahwe. 8 Kwa hiyo mfalme aliamuru,
na wakatengeneza kasha na kulileta nje kwenye lango kwenye nyumba ya Yahwe.
9 Kisha wakafanya tangazo katika Yuda na Yerusalemu, kwa ajili ya watu kuleta kwa
Yahwe kodi aliyoiagiza Musa mtumishi wa Mungu juu ya Israeli jangwani. 10 Viongozi
wote na watu wote wakafurahia na wakaleta fedha na kuiweka kwenye kasha hadi
walipomaliza kulijaza. 11 Ikatokea kwamba kila lilipoletwa kasha kwa mikono ya
Walawi kwa wakuu wa mfalme, na kila walipoona kwamba kulikuwa na fedha
nyingi sana ndani yake, waandishi wa mfalme na mkuu wa kuhani mkuu walikuja,
kulihamishia fedha kasha, na kulirudisha sehemu yake. Walifanya hivyo siku baada
siku, wakikusanya kiasi kikubwa cha fedha. 12 Mfalme na Yehoyada akawapa zile
fedha wale waliofanya kazi ya kuhudumu katika nyumba ya Yahwe, Watu hawa
waliwaajiri waashi na maseremala ili waijenge nyumba ya Yahwe, na pia wale
waliofanya kazi katika chuma na shaba. 13 Kwa hiyo wafanya kazi wakafanya kazi,
na kazi ya kukarabati ikasonga mbele mikononi mwao; waakaisimamisha nyumba
ya Mungu katika hali yake halisi na kuiimarisha. 14 Walipomaliza, wakaleta fedha
zilizobaki kwa mfalme na Yehoyada. Fedha hizo zilitumika kutengenezea samani
kwa ajili ya nyumba ya Yahwe, vyombo vya huduma na kutolea dhabihu—vijiko na
vyombo vya dhahabu na fedha. Wakatoa sadaka za kuteketezwa bila kukomaa katika
nyumba ya Yahwe kwa siku zote za Yehoyada. 15 Yehoyada akazeeka na alaaikuwa
amejaa siku, na kisha akafa; alikuwa na umri wa mika 130 alipokufa. 16 Wakamzika
katika aamji wa Daudi miongoni mwa wafalme, kwa sababu alikuwa amefanya mema
katika Israeli, kwa Mungu, na kwa ajili ya nyumba ya Mungu, 17 Sasa baada ya
kifo cha Yehoyada, kiongozi wa Yuda akaja na kutoa heshima kwa mfalme. Kisha
mfalme akawasikiliza. 18 Wakaiacha nyumba ya Yahwe, Mungu wa babu zao, na
kuwaabudu miungu na maashera na sanamu. Ghadhabu ya Mungu ikaja juu ya
Yuda na Yerusalemu kwa sababau ya hili kosa lao. 19 Bado akatuma manabii kwao
ili kuwaleta tena kwake, Yahwe, manabii wakatangaza juu ya watu, lakini walipuuza
kusikiliza. 20 Roho wa Mungu akaja juu ya Zekaria mwana wa Yehoyada, yule kuhani;
Zekaria akasimama juu ya watu na kusema kwao, "Mungu anasema hivi: Kwa nini
mnazivunja amri za Yahwe, ili kwamba msifanikiwe? Kwa kuwa mmemsahau Yahwe,
pia amewasahau ninyi." 21 Lakini wakapanga njama dhidi yake; kwa amri ya mfalme,
wakampiga kwa mawe katika uwanja wa nyumba ya Yahwe. 22 Katika namna hii
hii, Yoashi, yule mfalme, akapuuza ukarimu ambao Yehoyada, baba yake Zekaria,
alikuwa amemfanyia. 23 Ikawa karibu mwisho wa mwaka, kwamba jeshi la Aramu
wakaja juu yake Yoashi. Wakaja Yuda na Yerusalemu; wakawaua viongozi wote wa
watu na kupeleka nyara zote kutoka kwao kwa mfalme wa Dameski. 24 Jeshsi la
Waaramu walikuwa wamekuja na jeshi dogo, lakini Yahwe akawapa ushindi juu ya
jeshi kubwa, kwa sababu Yuda alikuwa amemsahau Yahwe, Mungu wa babu zao.
Katika namna hii Waaramu wakaleta hukumu juu ya Yoashi. 25 Katika muda ambao
Waaramu walikuwa wameondoka, Yoashi alikuwa amejeruhiwa vikali. Watumishi
wake wakapanga njama dhidi yake kwa sababu ya mauaji ya wana wa Yehoyada,
yule kuhani. Wakamuua katika kitanda chake, na akafa; wakamzika katika mji wa
Daudi, lakini siyo katika makaburi ya wafalme. 26 Hawa walikuwa watu waliopanaga
njama dhidi yake: Zabadi mwana wa Shimeathi, Mwamoni; na Yehozabadi mwana

wa Shimrithi, Mwanamke Mmoabu. [27] Sasa matukio kuhusu wanaye, unabii muhimu uliokuwa umesemwa kumhusu yeye, na kujengwa tena kwa nyumba ya Mungu, ona, yameandikwa katika Kamusi ya kitabu cha wafalme. Amazia mwanaye, akawa mfalme katika nafasi yake.

# 25

[1] Amaza alikuwa na umri wa amiaka ishirini na na tano alipoanza kutawala;
alitawala miaka ishini na tisa katika Yerusalemu. Jina la mama yake lilikuwa
Yehoadani, wa Yerusalemu. [2] Alifanya yaliyokuwa sahihi katika macho ya Yahwe,
lakini siyo kwa moyo uliojitoa kikamilifu. [3] Ikawa kwamba mapema utawala wake
ulipokuwa umeimarika, aliwaua watumishi ambao walikuwa wamemuua baba yake,
mfalme. [4] Lakini hakuwaua watoto wa wale wauaji, bali alitenda kama kama
ilivyoaandikwa katika sheria, katika kitabu cha Musa, kama Yahwe alivyokuwa
ameamru. "Baba hatajuta kwa ajili ya watoto, wala watoto hawatakufa kwa
ajili ya baba zao. Badala yake, kila mtu lazima afe kwa ajili ya dhambi zake
mwenyewe". [5] Aidha, Amazia aliwakusanya Yuda pamoja, na akawaandikisha
kwa kufuata nyumba za babu zao, chini ya maakida wa maelfu na maakida wa
mamia —wote wa Yuda na wa Benyamini. Akawahesabu kuanzia wa mika ishirini
na kuendelea, na akawaona wako 300, 000 wanaume waliochaguliwa, wawezaoa
kwenda vitani, walioweza kushika mkuki na ngao. [6] Pia alikodi wanaume wa
kupigana 100, 000 kutoka Israeli kwa fedha mia moja. [7] Lakini mtu wa Mungu alikuja
kwake na kusema, " Mfalme, usiliache jeshi la Istaeli kwenda nawe, kwa maana
Yahwe hayupo pamoja na Israeli -wala na mtu Yeyote wa Efraimu. [8] Lakini hata
kama mtaenda na mkiwa wenye ushupavu na imara katika vita, Mungu atawatupa
chini mbele ya adui, kwa maana Mungu ana nguvu za kusaidia, na nguvu za kurusha
chini". [9] Amazia akasema kwa mtu wa Mungu, "Lakini tutafanyaje kuhusu talanta
mia moja nilizowapa jeshi la Israeli? Mtu wa Mungu akajibu, Yahwe anauwezo
wa kukupa vingi zaidi kuliko hivyo." [10] Kwa hiyo Amazia akalitenganisha jeshi
lilokuja kwake kutoka Efraimu; akawarudisha nyumbani tena. Hivyo hasira yao
iliwaka sana zidi ya Yuda, na walirudi nyumbani kwa hasara kali. [11] Amazia
akajipa ujasiri na kuwaongoza watu wake kwenda nje kwenye bonde la chumvi,
huko akawashinda wanaueme elfu kumi wa Seiri. [12] Jeshi la Yuda likawachukua elfu
kumi wengine wakiwa hai. Wakawapeleka juu ya mwamba na kuwarushwa chini
kutoka huko, hivyo wote wakavunjika vunjika katika vipande. [13] Lakini watu wa
jeshi ambalo Amazia alilirudisha, ili kwamba wasiende naye vitani, wakauvamia mji
Yuda kuanzia Somaria hadi Beth- horoni. Wakawapiga watu elfu tatu na kuwateka
wengi sana. [14] Sasa ikawa kwamba baada ya Amazia kurudi kutoka kuwachinja
Waedomu, akaileta miungu ya watu wa Seiri, na kuisimamisha iwe miungu yake.
Akainama chini mbele ya hiyo miungu na kuitolea sadaka za uvumba. [15] Hivyo hasira
ya Yahwe ikawaka zidi ya Amazia. Akamtuma nabii kwake, ambaye alisema, "Kwa
nini umeitafuta miungu ya watu ambayo haikuwaokoa hata watu wake yenyewe
zidi ya mkono wako?" [16] Akiwa kwamaba yule nabii alipokuwa anaongea naye,
mfalme akamwambia, "Je, wewe tumekufanya kuwa mshauri wa mfalme? Acha!
Kwa nini ujitakie kuuawa?" Kisha nabii akaacha na kusema, ninajua kwamba
Mungu ameamua kukuangaamiza kwa sababu umefanya tendo hili na hujasikilisa
ushauri wangu." [17] Kisha Amazia akashauriana na washauri na kutuma wajumbe
kwa Yehoashi mwana wa Yehoahazi mwana wa Yehu, mfalme wa Israel. akisema,
"Njoni, tukutane uso kwa uso katika vita". [18] Lakini Yehoashi mfalme wa Israeli
akatuma wajumbe kwa Amaziahi mfalme wa Yuda, akisema, Mbaruti uliokuwa
Lebanoni ulituma ujumbe kwa mwerezi ulioko Lebanoni, ukisema, Mtoe binti yako

kwa mwanangu awe mke wake; lakini akapita hayawani katika Lebanoni akatembea
na kuukanyaga chini mbaruti. 19 Umesema, 'Ona, nimeipiga Edomu,' na moyo wako
umekuinua juu. Jipe fahari katika ushindi wako, lakini ukae nyumbani, kwa maana
ni kwa nini ujisababishie matatizo mwenyewe na kuanguka, wote wewe na Yuda
pamoja nawe?' 20 Lakini Amazia hakusikiliza, kwa sababu tukio hili lilikuwa limetoka
kwa Mungu, ili awatie Waisraeli katika mkono wa adui zao, kwa sababu walikuwa
wametafuta ushauri kutoka kwa miungu ya Edomu. 21 Kwa hiyo, Yehoashsi, mfalme
wa Israeli, akavamia; yeye na Amazia, mfalme wa Yuda, wakakutana uso kwa uso
huko Beth -shemishi, ulioko Yuda. 22 Yuda akashindwa mbele za Israeli, na kila mtu
akarudi nyumbani. 23 Yehoashi, mfalme wa Israeli, akamkamata Amazia mwana
wa Yehoashi mana wa Ahazia, mfalme wa Yuda, huko Beth - shemeshi. Akamleta
Yerusalemu na kuuangusha chini ukuta wa Yerusalemu kuanzia Lango la Efraimu
hadi kona ya Lango, umbali wa mikono mia nne. 24 Akachukua dhahabu na fedha
zote, vitu vyote vilivyoonekana akatika nyumba aya Mungu kwa Obedi Edomu, na
vitu vya thamanai katika nyumba ya mfalme, na mateka pia, na akarudi Samaria.
25 Amazia mwana wa Yoashi, mfalme wa Yuda, aliishi miaka kumi na tano baada
ya kifo cha Yehoashi, mwana wa Yehoahazi, mfalme wa Israeli. 26 Kwa mambo
mengingine kuhusu Amzia, mwanzo na mwisho, tazama, je, hayajaandikwa katika
kitabu cha wafalme wa Israeli? 27 Sasa kutoka wakati amabaoa Amazia aligeukia
mbali asimfuate Yahwe, walianza kupanga njama zidi yake katika Yerusalemu.
Akakimbilia Lachishi, lakini wakatuma watu nyuma yake wamfuate Lachishsi na
walimuua huko. 28 Wakamleta juu ya farasis na wakamzika pamoja na babu zake
kataika Mji wa Yuda.

# 26

1 Watu wote wa Yuda wakamchukua Uzia, ambaye alikuwa na aumri wa mika
kumi na sita, na wakamfanya mfalme katika nafasi ya baba yake Amazia. 2 Ndiye
aliuyeijenga tena Elathi na kuurejesha kwa Yuda. Baada ya hapo mfalme akalala
pamoja na babu zake. 3 Uzia alikuwa na umri wa miaka kumi na sita alipoanza
kutawala. Akatawala miaka ishirini na mabili katika Yerusalemu. Jina la mama
yake lilikuwa Yekolia; alikuwa wa Yerusalemu. 4 Akafanya yaliyokuwa sahihi katika
macho ya Yahwe, akiufuata mfano wa baba yake, katika kila jamabo. 5 Alijitoa
kumtafuta Mungu katiaka siku za Zekaria, ambaye alimpa maelekezo kwa ajili ya
kumtii Mungu. Kadri alivyomtafuta Yaahwe, Mungu alimfanikisha. 6 Uzia akaenda
na kupigana zidi ya Wafilisti. Akaubomoa ukuta wa mji wa Gathi, Yabne, na
Ashdodi; akajenga miji katika nchi ya Ashdodi na miongoni mwa Wafilisti. 7 Mungu
aakaamsaidia zidi ya Wafilist, zidi ya Waarabu waliokuwa wakiishi Gur - baali, na
zidi ya Wameuni. 8 Waamoni wakalipa kodi kwa Uzia, na umaarufu wake ukaenea,
hata kufika maingilio ya Misiri, kwa sababu alikuwa ameanza kuwa maarufu. 9 Zaidi
ya hayo, Uzia akajenga minara katika Yerusalemu katika kona ya Lango, kwenye
Lango la Bonde, na pa kwenye kona ya ukuta, na akavizungushia ngome. 10 Akajenga
minara ya ulinzi katika nyika na akachimba mabwawa, kwa maana alikuwa na
ng'ombe wengi, katika visiwa vya chini na katika nchi tambarare. Alikuwa na
wakulima na wapandaji wa zabibu katika mwinuko wa nchi na katika mashamba
yenye rutuba, kwa maana alipenda kulima. 11 Zaidi ya hayo, Uzia alikuwa na jeshi
la wanaume wa kupigana vita ambao walienda vitani katika makundi ambayo idadi
yake ilikuwa imehesabiwa na Yeieli, mwandishi. na Maaseya, afisa, chini ya mamlaka
ya Hanania, mmoja wa maamri jeshi wa mfalme. 12 Jumla ya wakuu wa nyumba za
mababu, watu wa kupigana vita, walikuwa 2, 600. 13 Chini ya mkono wao kulikuwa
na jeshi la watu 307, 500 ambao walifanya vita kwa nguvu ili kumsaidia mfalme

idi ya maadui. 14 Uzia akaandaa kwa ajili yao—kwa ajili ya jeshi lote — ngao,
mikuki, chapeo, deraya za majini, nyuta, na mawe ya kurusha. 15 Katka Yerusalemu
alijenga mitambo, iliyobuniwa na watu wenye ujuzi, ili iwe juu ya minara na juu ya
buruji, kwa ajili ya kurushia mishale na mawe makaubwa. Umaarufu wake ukaenea
hadi nchi za mbali, kwa maana alisaidiwa sana hadi alipokuwa na ngavu sana.
16 Lakini Uzia alipokuwa amekuwa na nguvu nyingi, moyo wake ulijiinua akatenda
kwa uovu; akafanya makosa zidi ya Yahwe, Mungu wake, kwa maana aliendakwenye
nyumba ya Yahwe kwa ajili ya kufukiza uvumba juu ya madhabahu ya kufukizia.
17 Azaria, kuhani, akamfuata, na pamoja naye makuhanai themanini wa Yahwe,
ambao walikuwa watu wenye ujasiri. 18 Walimzuia Uzia, mfalme, na wakasema
kwake, " Siyo jukumu lako, Uzia, kumtolea Yahwe uvumba, bali ni kazi ya makuhani,
wana wa Haruni, amabao wametengwa kwa ajili ya kutoa sadaka za uvumba. Toka
nje ya sehemu takatifu, kwa maana huna uaminifu na hautaheshimiwa na Yahwe
Mungu." 19 Kisha Uzia akakasirika. Alikuwa ameshikilia chetezo mkononi kwa ajili
ya kufukiza uvumba. Wakati alipowaghadhabikia makuhani, ukoma ukatokea juu ya
uso wake mbele ya makuhani katika nyumba ya Yahwe, pembeni mwa madhabahu
ya uvumba. 20 Azaria kuhani mkuu na makuhani wote wakamwanagalia, na, tazama,
alikuwa amepatwa ukoma juu ya uso wake. Walimwondoa pale haraka. Kwa
hakika, aliharakisha kwenda nje, kwa maana Yahwe alikuwa amempiga. 21 Uzia,
mfalme, alikuwa mwenye ukoma hadi siku ya kufa kwake na aliishi katika nyumba
ya kutengwa tangu alipokuwa mwenye ukoma, kwa maan alitengwa na nyumba ya
Yahwe. Yothamu, mwanaye, alikuwa mkuu wa anyumba ya mfalme na aliwatawala
watu wa nchi. 22 Mambo mengine kuhusu Uzia, mwanzo na mwisho, yako katika
kile ambacho Isaya, mwana wa Amozi, nabii, aliandika. 23 Kwa hiyo Uzia akalala
pamoja na babu zake; walimzka pamoja na babu zake katika uwanja wa maziko wa
Mfalme, kwa maana walisema, "Ni mwenye ukoma". Yothamu, mwanaye, akawa
mfalme katika nafasi yake.

# 27

1 Yothamu alikuwa na umri wa mika ishirini na mitano alipoanza kutawala;
alitawala miaka kumi na sita katika Yerusalemu. Jina la mama yake lilikuwa Yerusha;
alikuwa binti Sadoki. 2 Akafanya yaliyomema katika macho ya Yawe, akiufuta mfano
wa baba yake, Uzia, katika mabo yote. Pia alijiepusha kuingia katika hekalu la Yahwe.
Lakini watu bado walikuwa wanaenda katika njia za uovu. 3 Akalijenga tena lango
la juu la nyumba ya Yahwe, na juu ya kilima cha Ofeli akajenga sana. 4 Vilevile
alijenga miji katika kilima cha Yuda, na katika mistu alijenga ngome na minara. 5 Pia
alipigana na mfalme wa watu wa Amoni na akawashinda. Katika mwaka huo huo,
watu wa Amoni walimpa talanta mia moja za fedha, kori elfu kumi za ngano, kori
elfu kumi za shayiri. Watu wa Amoni wakampa hivyo hivyo katika mwaka wa pili
na wa tatu. 6 Kwa hiyo Yothamu akawa na nguvu sana kwa sababu alitembea imara
mbele za Yahwe Mungu wake. 7 Kwa mambo mengine kuhusu Yothamu, vita vyake
vyote, na njia zake zote, ona, yameandikwa katika kitabu cha wafalme wa Israeli na
Yuda. 8 Alikuwa na umri wa miaka ishirini na mitano alipoanza kutawala; alitawala
kwa miaka kumi na sita kataika Yerusalemu. 9 Yothamu akalala pamoja na babu
zake, na wakamzika katika mji wa Daudi. Ahazi, mwanaye, akawa mfalme katika
nafasi yake.

# 28

1 Ahazi alikuwa na umri wa miaka ishirini na mitano alipoanza kutawala, na
akatawala miaka kumi na sita katika Yerusalemu. Hakufanya yaliyoadili katika

macho ya Yahwe, kama Daudi babu yake alivyokuwa amefanya. 2 Badala yake,
alitembea katika njia za wafalme wa Israeli; pia alitengeneza sanamu za kusubu kwa
ajila ya Mabaali. 3 Zaidi ya hayo, akafukiza uvumba katika bonde la Beni Hinomu
na akawaweka watoto wake ndani ya moto, kwa mjibu wa desturi za uzinzi za watu
ambao Yahwe aliwafukuza nje ya nchi zao mbele za watu wa Israeli. 4 Akatoa sadaka
na kufukiza uvumba katika sehemu za juu na juu ya vilima na chini ya kila mti wenye
majani mabichi. 5 Kwa hiyo Yahwe Mungu wa Ahazi, akamweka katika mikono
ya mfalme wa Shamu. Waaramu wakamshinda na kuchukua kutoka kwake kundi
kubwa la mateka, wakawapeleka Damesiki. Ahazi pia aliwekwa katika mikono ya
mfalme wa Israeli ambaye alimshinda kwa mauji makuu. 6 Kwa maana Peka mwana
wa Remalia, aliwaua katika Yuda wanajeshi 120, 00 kwa siku moja, wote walikuwa
wanaume hodari, kwa maana walikuwa wamemsahau Yahwe, Mungu wa babu zao.
7 Zikri, mtu mwenye nguvu kutoka Efraimu, akawaua Maaseya mwana wa mfalme,
Azrikamu, mwangalizi mkuu wa ikulu, na Elkana, ambaye alikuwa karibu na mfalme.
8 Jeshsi la Israeli likachukua mateka kutoka kwa ndugu zao 200, 000 wake, wana,
na mabinti. Pia wakachukua nyara nyingi, ambazo walipeleka Samaria. 9 Lakini
nabii wa Yahwe alikuwapo huko, jina lake aliitwa Odedi. Alikwenda nje kukutana
na jeshi likiingia Samaria. Akawaambia, “Kwa sababu Yahwe, Mungu wa babu zenu,
alikuwa na hasiri na Yuda, akawatia katika mikono yenu. Lakini mmewaua katika
hasira inayofika juu mbinguni. 10 Sasa ninyi badala ya kuwahifadhi wanaume na
wanawake wa Yuda na Yerusalemu kama watumwa wenu. Lakini je hamko na hatia
ya dhambi zenu zidi ya Yahwe Mungu wenu? 11 Sasa basi, nisikilizeni: warudisheni
wafubgwa, ambao mmewachukua wa ndugu zenu, kwa maana ghadhabu ya Yahwe
iko juu yenu.” 12 Kisha baadhi ya viongozi wa watu wa Efraimu—Azaria mwana wa
Yohanani, Berekia mwana wa Meshiremothi, na Yehizikia mwana wa Shalumu, na
Amasa mwana wa Hadlai, wakasimama kinyume na wale waliorudi kutoka vitani.
13 Wakasema kwao, “Lazimaa msiwaleta wafungwa hapa, kwa kuwa mlikusudia
jambo ambalo litaleta juu yetu dhambi dhidi ya Yahwe, kuongeza dhambi juu
yetu na makosa yetu, kwa maana makosa yetu ni makuu, na kuna hasira kali
dhidi ya Israeli.” 14 Hivyo watu wenye silaha wakawaacha wafungwa na mateka
mbele ya viongozi wa Israeli na kusanyiko lote 15 Watu ambao walipangwa kwa
majina wakanyanyuka na kuwachukua wafungwa, na kuwavika wote waliokuwa
uchi miongoni mwa mateka. Wakawavika na kuwapa viatu. Wakawapa chakula wale
na kunywa. Wakawahudumia majeraha yao na kuwaweka waliodhaifu juu ya punda.
Wakawarudisha kwenye familia zao katika Yeriko, (Ulioitwa mji wa mitende). Kisha
wakarudi Samaria. 16 Wakati huo Mfalme Ahazi akatuma wajumbe kwa wafalme
wa Ashuru kuwaomba wamsaidie. 17 Kwa maana Waedomu walikuwa wamekuja
tena na kuvamia Yuda, wakachukua wafungwa. 18 Wafilisti pia wakavamia miji
ya nchi ya chini na ya Negebu ya Yuda. Waliichukua Beth-shemeshi, Ayaloni,
Giderothi, SoKo pamoja na vijiji vyake, Timna pamoja na vijiji vyake. Wakaenda
kuishi katika sehemu hizo. 19 Kwa kuwa Yahwe aliishusha chini Yuda kwa sababu
ya Ahazi, mfalme wa Israeli; kwa maana alikuwa ametenda maovu katika Yuda na
alikuwa ametenda dhambi nzito sana dhidi ya Yahwe. 20 Tiglath-pileseri, mfalme
wa Ashuru, akaja kwake na akampa tabu badala ya kumpa nguvu. 21 Kwa kuwa
Ahazi aliteka nyara nyumba ya Yahwe na nyumba ya mfalme na viongozi, kwa
ajili ya kuvitoa vitu vya thamani kwa mfalme wa Ashuru. Lakini kufanya hivyo
hakukumfaidisha yeye. 22 Mfalme Ahazi huyu huyu akatenda dhambi hata zaidi
dhidi ya Yahwe katika muda wa mateso yake. 23 Kwa maana aliwatolea dhabihu
mingu wa Dameski, miungu ambao walimshinda. Akasema, “Kwa sababu miungu
wa mfalme wa Aramu waliwasaidia, nitawatolea sadaka ili wanisaidie.” Lakini

walikuwa watesi wake na Israeli yote.
[24] Ahazi akazikusanya pamoja samani za
nyumba ya Mungu na kuzikata vipande vipande. Akaifunga milango ya nyumba
ya Yahwe na kuzitengeneza madhabahu kwa ajili yake mwenyewe katika kila kona
ya Yerusalemu.
[25] Katika kila mji wa Yuda akafanya sehemu za juu kwa ajili ya
kutolea sadaka za kuteketezwa kwa miungu wengine. Akamfanya Yahwe, Mungu wa
babu zake, akasirike.
[26] Sasa matendo yake yaliyobaki, na njia zake zote, mwanzo na
mwisho, ona, yameandikwa katika kitabu cha wafalme wa Yuda na Israeli.
[27] Ahazi
akalala pamoja na babu zake, na wakamzika katika mji, katika Yerusalemu, lakini
hawakumleta kwenye makaburi ya wafalme wa Israeli. Hezekia, mwanaye, akawa
mfamle katika nafasi yake.

# 29

[1] Hezekia alianza kutawala alipokuwa na umri wa miaka ishirini na mitano;
alitawala miaka ishini na nane katika Yerusalemu. Jina la mama yake aliitwa Abiya;
alikuwa binti wa Zekaria.
[2] Alifanya yaliyoadili katika macho ya Yahwe, kama
Daudi baba yake alivyofanya.
[3] Katika mwaka wa kwanza wa utawala wake, katika
mwezi wa kwanza, Hezekia aliifungua milango ya nyumba ya Yahwe na kuikarabati.
[4] Akawaleta ndani makuhani na Walawi, na akawakusanya pamoaja katika uwanda
upande wa mashariki.
[5] Akawaambia, “Nisikilizeni, ninyi Walawi! Jitakaseni
wenyewe, na itakaseni nyumba ya Yahwe, Mungu wa babu zenu, na uondoeni mbali
uchafu kutoka kwenye sehemu takatifu.
[6] Kwa kuwa babu zetu walikosea na kufanya
kilichokuwa uovu katika macaho ya Yahwe Mungu wetu; walimsahau, wakageuzia
mbali nyuso zao kutoka sehemu ambapo Yahwe anaishi, na kuigeuzia migongo yao.
[7] Pia waliifunga milango ya ukumbi nakuziweka nje taa; hawakufukiza uvumba au
kutoa sadaka za kuteketezwa katika sehemu takatifu kwa Mungu wa Israeli.
[8] Kwa
hiyo hasira ya Yahwe ilikuwa imeshuka juu ya Yuda na Yerusalemu, na amewafanya
kuwa kitu cha wasiwasi, cha hofu, na cha kudharauriwa, kama mnavyoona kwa
macho yenu.
[9] Hii ndiyo maana mababu zetu wameanguka kwa upanga, na wana
wetu, binti zetu, na wake zetu wako katika utumwa kwa sababu ya hili.
[10] Sasa ni
katika moyo wangu kufanya agano na Yahwe, Mungu wa Israeli, ili kwamba hasira
yake kali iweze kugeukia mbali nasi.
[11] Wanangu, msiwe wavivu sas, kwa kuwa
Yahwe amewachagua kwa ajili ya kusimama mbe yake, kwa ajili ya kumwabudu yeye,
na kwamba muwe watumishi wake na kufukiza uvumba.”
[12] Basi Walawi wakainuka;
Mahathi mwana wa Amasai, na Yoeli mwana wa Azaria, wa watu wa Kohathi; na
wa watu wa Merari, Kishi mwana wa Abdi, na Azaria mwana wa Yehaleleli; na wa
Wargeshoni, Yoa mwana wa Zimna, na Edeni mwana wa Yoa;
[13] wa wana wa Elisafani,
Shimri na Yeueli; wa wana wa Asafu, Zekaria na Matania;
[14] wa wana wa Hemani,
Yehueli na Shimei; na wa wana Yeduthuni, Shemaya na Uzieli.
[15] Wakawakusanya
ndugu zao, wakajitakasa wenyewe, na wakaenda ndani, kama alivyoamru mfalme,
wakifuata maneno ya Yahwe, kwa ajili ya kuisafisha nyumba ya Yahwe.
[16] Makuhani
wakaenda kwenye sehemu za ndani ya nyumba ya Yahwe kwa ajili ya kuisafisha;
wakaleta nje uchafu wote walioukuta ndani ya hekalu la Yahwe katika uwanja wa
nyumba. Walawi wakauchukua kuubeba nje ya hadi kwnye kijito cha Kidroni.
[17] Sasa
wakaanza utakaso katika siku ya kwanza ya mwezi. Katika siku ya nane ya mwezi
wakaufikia ukumbi wa Yahwe. Kisha siku nane zaidi wakaitakasa nyumba ya Yahwe.
Katika siku ya kumi na sita ya mwezi wa kwanza wakamaliza.
[18] Kisha wakaenda
kwa Hezekia, mfalme, ndani ya ikulu na kusema, “Tumeisafisha nyumba yote ya
Yahwe, madhabahu kwa ajili ya kutolea sadaka za kuteketezwa pamoja na vifaa
vyake vyote, na meza ya mkate wa uwepo, pamoja na vifaa vyake vyote.
[19] Kwa
hiyo tumejiandaa na tumevitakasa vitu vyote ambavyo Mfalme Ahazi aliviondoa

wakati alipoenda kwa ukengeufu katika kipindi cha utawala wake, ona, viko mbele
ya madhabahu ya Yahwe." 20 Kisha Hezekia mfalme akaamka mapema asubuhi na
kuwakusanya viongozi wa miji; akaenda kwenye nyumba ya Yahwe. 21 Wakaleta
ng'ombe waume saba, kondoo waume saba, wanakondoo saba, mbuzi waume saba
kama sadaka ya dhambi kwa ajili ya mfalme, kwa ajili ya patakatifu, kwa ajili ya
Yuda. Akawaamuru makuhani, wana wa Haruni, kuwatoa sadaka juu ya madhabahu
ya Yahwe. 22 Kwa hiyo wakawachinja ng'ombe, na makuhani wakaipokea damu
na kuinyunyiza juu ya madhabahu. Wakawachinja kondoo dume, na kunyunyiza
damu juu ya madhabahu; Pia wakawachinja wanakondoo na kuinyunyiza damu
juu ya madhabahu. 23 Wakawaleta mbuzi kwa ajili ya sadka ya dhambi mbele
ya mfalme na kusnyiko; wakaweka mikono yao juu ya hao mbuzi. 24 Makuhani
wakawachinja, na wakafanya sadaka ya dhambi kwa damu yao juu ya madhabahu ili
kufanya upatanisho kwa ajili ya Israeli wote, kwa maana mfalme alikuwa ameamuru
kuwa sadaka ya kuteketezwa na sadaka ya dhambi lazima zifanywe kwa ajili ya
Israeli wote. 25 Hezekia akawaweka Walawi katika nyumba ya Yahwe wakiwa na
matoazi, vinanda, na vinubi, akiwapanga kwa amri ya Daaudi, Gadi, mwonaji wa
mfalme, na Nathani, nabii, kwa maana amri ilitoka kwa Yahwe kupitia manabii
wake. 26 Walawi wakasimama na vyombo vya Daudi, na makauhani wakasimama
na matarumbeta. 27 Hezekia akawaamuru kutoa sadaka za kuteketezwa juu ya
madhabahu. Sadaka zilipoanza, wimbo wa Yahwe ukaanza pia, kwa matarumbeta,
pamoja na vyombo vya Daudi, mfalme wa Israeli. 28 Kusanyiko lote wakaabudu,
waimbaji wakaimba, na wapiga matarumbeta wakapiga; yote hayo yakaendele hadi
sadaka za kuteketezwa zilizipokwisha. 29 Walipomaliza kutoa sadaka, mfalme na
watu waliokuwepo pamoja naye wakainama, na kusujudu. 30 Vile vile, Hezekia,
mfalme, na viongozi wakawaamuru Walawi kuimba ili kumsifu Yahwe kwa maneno
ya Daudi na ya Asafu, mwonaji. Wakaimba sifa kwa furaha, wakainama chini
wakasujudu. 31 Kisha Hezekia akasema, "Sasa mmejiweka wakfu wenyewe kwa
Yahwe. Njoni hapa na mlete sadaka na dhabihu za shukrani katika nyumba ya
Yahwe." Kusanyiko wakaleta sadka na dhabihu za shukrani, na wote waliaokuwa
na moyo wa kuhiyalika wakaleta sadka za kuteketezwa. 32 Hesabu ya sadaka za
kuteketezwa ambazo kusanyiko walileta ilikuwa ng'ombe sabini, kondoo waume mia
moja, na wanakondo waume mia mbili. Wote hao walikuwa kwa ajili ya sadaka za
kuteketezwa kwa Yahwe. 33 Sadaka za kuwekwa wakfu zilikuwa ng'ome mia sita na
kondoo elfu tatu. 34 Lakini makuhani walikuwa wachache sana kuchuna sadaka zote
za kuteketezwa, kwa hiyo ndgugu zao, Walawi, wakawasaidia hadi kazi ilipoisha,
na hadi makuhani walipoweza kujitakasa wenyewe, kwa maana Walawi walikuwa
makaini sana kujitaksa wenyewe kuliko makuhani. 35 Zaidi ya hayo, palikuwa na
sadaka za kuteketezwa nyingi sana; zilitolewa pamoja na sadaka za mafauta za
amani, na kulikuwa na sadaka za vinywaji kwa kila sadaka ya kuteketezwa. Kwa hiyo
huduma ya nyumba ya Yahwe ikawekwa katika utaratibu. 36 Hezekia akafurahia, na
watu pia, kwa sababu ya kile ambacho Mungu alikuwa ameandaa kwa ajili ya watu,
kwa maana kazi ilikuwa imekamilika haraka.

# 30

1 Hzekia akatuma wajumbe kwa Israeli wote na Yuda, na pia akawaandikia
barua Efraimu na Manase, kwamba waje kwenye nyumba ya Yahwe katika
Yerusalemu, kusherekea Pasaka ya Yahwe, Mungu wa Israeli. 2 Kwa maana mfalme,
viongozi wake, na kusanyiko lote katika Yerusalemu walikuwa wameshauriana
pamoja, wakakubaliana kusherekea Pasaka katika mwezi wa pili. 3 Hawakuweza
kuisherekea mapema kabla ya hapo, kwa sababu hapakuwa na makuhani wa kutosha

waliojitakasa wenyewe, wala watu hawakuwa wamekusanyika pamoja Yerusalemu.
4 Pendekezo hili likaonekana sahihi katika macho ya mfalme na ya kusanyiko lote.
5 Kwa hiyo wakakubaliana kufanya tangazo katika Israeli yote, kuanzia Beer-sheba
hadi Dani, kwamba watu lazima waje kusherehekea Paska ya Yahwe, Mungu wa
Israeli, huko Yerusalemu. Kwa maana walikuwa hawakuwa wameisherehekea kwa
hesabu kubwa ya watu, kwa mujibu wa jinsi ilivyokuwa imeandikwa. 6 Hivyo
matarishi wakaenda na barua kutoka kwa mfalme na viongozi wake katika Israeli
na Yuda yote, kwa agizo la mfalme. wakasema, "Ninyi watu wa Israeli, rudini
kwa Yahwe, Mungu wa Abrahamu, Isaka na Israeli, ili kwamba aweze kuwarudia
masalia wenu ninyi mlipona kutoka kwenye mkono wa wafalme wa Ashuru. 7 Msiwe
kama babu zenu au ndugu zenu, ambao walimuasi Yahwe, Mungu wa mababu zao,
hivyo akawaweka katika kuangamia, kama mnavyoona. 8 Sasa msiwe wasumbufu,
kama babu zenu walivyokuwa; badala yake, jitoeni wenyewe kwa Yahwe na njoeni
kwenye sehemu yake takatifu, ambayo ameitakasa milele, na mwabuduni Yahwe
Mungu wenu, ili kwamba uso wake wenye hasira uwageukie mbali. 9 Kwa maana
ikiwa mtageuka nyuma kwa Yahwe, ndugu zenu na watoto wenu watapata huruma
mbele ya hao wanaowaongoza kama wafungwa, na watarudi katika nchi hii. Kwa
maana Yahwe Mungu wenu, ni mkarimu na mwenye huruma, na hatawageuzia
mbali uso wake, kama mtarudi kwake." 10 Kwa hiyo matarishi wakapita mji kwa
mji katika majimbo ya Efraimu na Manase, njia yote hadi Zabuloni, lakini watu
waliwacheka na kuwazomea. 11 Lakini, watu wengine wa Asheri na Manase na
Zabuloni walijinyenyekesha wenyewe na wakaja Yerusalemu. 12 Mkono wa Mungu
pia ukaja juu ya Yuda, kuwapa moyo mmmoja, ili kulikubali agizo la mfalme na
viongozi kwa neno la Yahwe. 13 Watu wengi, kusanyiko kubwa, likakusanyika
Yerusalemu kusherehekea Sikukuu ya Mikate Isiyochacha katika mwezi wa pili.
14 Waliinuka na kuchukua madhabahu zizilizokuwa Yerusalemu, madhabahu zote
kwa ajili ya sadaka za kufukiza; wakazirusha katika kijito Kidroni. 15 Kisha
wakamuua mwanakondoo wa Paska katika siku ya kumi na nne ya mwezi wa pili.
Makuhani na Walawi wakaona aibu, kwa hiyo wakajitakasa wenyewe na kuleta
sadaka za kuteketezwa katika nyumba ya Yahwe. 16 Wakasimama katika sehemu
zao katika makaundi yao, wakifuata maelekezo yaliyotolewa na sheria ya Musa, mtu
wa Mungu. Makuhani wakainyunyiza damu waliyoipokea kutoka kwenye mikono ya
Walawi. 17 Kwa maana walikuwepo wengi katika kusanyikao amaabao hawakuwa
wamejitakasa wenyewe. Kwa hiyo Makuhani wakamchinja mwanakondoo wa
Pasaka kwa ajili ya kila mmoja ambaye hakuwa amejisafisha na hakuweza kuzitakasa
sadaka zake kwa Yahwe. 18 Kwa kuwa wingi wa watu, wengi wao kutoka Efraimu
na Manase, Asakari na Zabuloni, hawakuwa wamejitakasa wenyewe, bado waliula
mlo wa Paska, kinyume na maelekezo yaliyoandikwa. Kwa kuwa Hezekia alikuwa
amewaombea, akisema, "Mungu Yahwe amsamehe kila mmoja 19 ambaye anaulekeza
moyo wake kumtafuta Mungu, Yahwe, Mungu wa babu zake, hata kama hajasafiswa
kwa utakaso wa viwango vya patakatifu." 20 Kwa hiyo Yahwe akamsikiliza Hezekia
na akawaponya watu. 21 Watu wa Israeli waliokuwepo Yerusalemu wakaitunza
Sikukuu ya Mikaate Isiyochachwa na furaha kubwa kwa siku saba. Walawi na
makuhani wakamsifu Yahwe siku baada ya siku, wakiimwimbia Yahwe kwa vyombo
vya sauti kuu. 22 Hezekia akazungumza kwa kuwatia moyo Walawi wote walioilewa
ibada ya Yahwe, Kwa hiyo wakala kwa kipindi cha siku saba, wakitoa sadaka za
amani, na kufanya toba kwa Yahwe, Mungu wa babu zao. 23 Kusanyiko lote kisha
likaamua kusherehekea kwa siku zingine saba, na wakafanya hivyo kwa furaha.
24 Kwa kuwa Hezekia mfalme wa Yuda aliwapa kusanyiko ng'ombe dume elf moja,
na kondoo elfu saba kama sadaka; na viongozi wakawapa kusanyiko ng'ombe dume

elfu moja na kondoo na mbuzi elfu kumi. Idadi kubwa ya makuhani wakajitakasa
wenyewe. 25 Kusanyiko lote la Yuda, pamoja na makuhani na Walawi na watu wote
walikuja pamoja kutoka nchi ya Israeli na wale walioishi Yuda—wote wakafurahia.
26 Hivyo kulikuwa na furaha kuu katika Yerusalemu, kwa kuwa tangu wakati wa
Solomoni mwana wa Daudi, mfalme wa Israeli, hapakuwa na kitu kama hicho katika
Yerusalemu. 27 Kisha makuhani, Walawi, wakainuka na kuwabariki watu. Sauti zao
zilisikika na maombi yao yakaenda juu mbinguni, sehemu takatifu ambapo Mungu
anaishi.

# 31

1 Sasa wakati haya yote yalipokwisha, watu wote wa Israeli waliokuwepo pale
wakaenda huko kwenye mji wa Yuda na wakazivunja vipande vipande nguzo
za mawe na wakazikata nchi za maashera, na wakazibomoa sehemu za juu na
madhabahu katika Yuda yote na Benyamini, na katika Efraimu na Manase, hadi
walipoziharibu zote. Kisha watu wote wa Israeli wakarudi, kila mtu kwenye
mali zake na kwenye mji wake. 2 Hezekia akayapanga makundi ya makuhani na
Walawi wakajipanaga kwa makundi yao, kila mtu akapangwa katika kazi yake, wote
makuhani na Walawi. Aliwapanga wafanye sadaka za kuteketezwa na sadaka za
amani, kuhudumu, kutoa shukrani, na kusifu katika malango ya hekalu la Yahwe.
3 Pia akawapanga katika sehemu ya mfalme kwa ajili ya sadaka za kuteketezwa
kutoka katika mali zake, hiyo ni kwa ajili ya, sadaka za kuteketezwa za asubuhi na
jioni, na sadaka za kuteketezwa kwa ajili ya siku za Sabato, mwezi mpya, na sikukuu
zisizobadilika, kama ilivyokuwa imeandikwa katika sheria ya Yahwe. 4 Vilevile,
akawaamuru watu walioishi Yerusalemu kutoa fungu kwa ajili ya makuhani na
Walawi, ili kwamba wawe makini katika kuitii sheria ya Yahwe. 5 Mapema mara
baada ya amri kutolewa, watu wa Israeli kwa ukarimu wakatoa malimbuko ya
nafaka, divai mpya, mafuta. asali, na kila kitu kutoka kwenye mavuno ya shamba.
Wakaleta ndani fungu la kumi la kila kitu; ambavyo vilikuwa kiasi kikubwa sana.
6 Watu wa Israeli na Yuda ambao waliishi katika mji wa Yuda pia wakaleta zaka za
ng'ombe na kondoo, na zaka za vitu vitakatifu amabavyo vilikuwa vimewekwa wakfu
kwa Yahwe Mungu wao, na wakavifunga katika marundo. 7 Ilikuwa mwezi wa tatu
wakati walipoanza kufunga michango yao katika marundo, na wakamaliza mwezi wa
saba. 8 Hezekia na viongozi walipokuja na kuyaona marundo, wakambariki Yahwe
na watu wake Israeli. 9 Kisha Hezekia akawauliza makuhani na Walawi kuhusu
marundo. 10 Azaria, kuhani mkuu, wa nyumba ya Zadoki, akamjibu na akasema,
“Tangu watu walipoanza kuleta matoleo katika nyumba ya Yahwe, tumekula na
tulikuwa navyo vya kutosha, tulibakiza vingi, kwa maana Yahwe amewabariki watu
wake. kilichokuwa kimebaki ni kiasi kikubwa hiki hapa.” 11 Kisha Hezekia akaagiza
vyumba vya kuhifadhia viandaliwe katika nyumba ya Yahwe, na wakaviandaa.
12 Kisha kwa uaminifu wakayaleta ndani matoleo, zaka, na vitu ambavyo ni vya
Yahwe. Konania, Mlawi, alikuwa meneja mkuu wa hivyo vitu, na Shimei, ndu yake,
alikuwa wa pili kwake. 13 Yehieli, Azaria, Nahathi, Asaheli, na Yerimothi, Yazabadi,
Elieli, Ismakia, Mahathi, na Benania walikuwa wasimamizi chini ya mkono wa
Konania na Shimei ndu yake, kwa uteuzi wa Hezekia, mfalme, na Azaria mwanagalizi
mkuu wa nyumba ya Mungu. 14 Kore mwana wa Imna Mlawi, bawabu katika
mlango wa mashariki, alikuwa juu ya sadaka za hiari za Mungu, msimamizi wa
kugawa sadaka kwa Yahwe na sadaka takatifu kuliko zote. 15 Chini yake walikuwepo
Edeni, Miniamini, Yoshua, Shemai, Amaaria, na Shekania, katika miji ya makuhani.
Wakazijaza ofisi za uaminifu, ili kutoa sadaka hizi kwa ndugu zao fungu kwa fungu,
kwa wote walio muhimu na wasiomuhimu. 16 Pia wakatoa kwa wale wanaume wenye
umri wa miaka mitatu na kuendelea, amabao walikuwa wameandikwa kataika

kaitatu cha babu zao walioiingia nyumba ya Yahwe, kwa mujibu wa ratiba ya kila
siku, kuifanya kazi katika ofisi zao na zamu zao. (Mandishi ya kale yanasema hivi:
“badala ya wanaume wa umri wa miaka mitatu na kuendelea”, wanaume wa mika
thelathini na kuendelea.”). [17] Waliwaganya makuhani kwa mujibu wa kumbu kumbu
za babu zao, na hivyo hivyo kwa Walawi wenye umri wa miaka ishirini na zaidi,
kwa mujibu wa ofisi zao na zamu zao. [18] Waliwajumuisha watoto wao wadogo
wote, wake zao, wana wao, na binti zao, katika jamii yote, kwa maana walikuwa
waaminifu katika kujitunza wenye watakatifu. [19] Kwa maana makuhani, uzao wa
Haruni, amabao walikuwa katika mashamba ya vijiji wakimilikiwa na miji yao, au
katika kila mji, palikuwa na watu walioteuliwa kwa majina kutoa mafungu kwa ajili
ya wanaume miongoni mwa makuhani, na kwa wote waliokuwa wameorodheshwa
katika kumbukumbu za babu zao kuwa miongoni mwa Walawi. [20] Hezekia alifanya
haya katika Yuda yote. Akakamilisha kilichokuwa chema, haki, na uaminifu mbele za
Yahwe Mungu wake. [21] Katika kila jambo ambalo alianzisha katika ibada ya nyumba
ya Mungu, sheria, na zile amri, kumtafuta Mungu, alikifanya kwa moyo wake wote,
na alifanikiwa.

# 32

[1] Baada ya mambo haya na matendo haya ya uaminifu, Senakeribu, mfalme
wa Ashuru, akaja na kuingia Yuda. Alipiga kambi kwa ajili ya kuivamia miji
yenye ngome, ambayo alikusudia kuiteka kwa ajili yake. [2] Sedekia alipoona
kwamba Senakeribu amekuja na kwamba amedhamiria kupigana zidi ya Yerusalemu,
[3] aliwashirikisha viongozi wake na watu wake wenye nguvu kuyazuia maji ya
chemichemi yaliyokuwa nje ya mji; waalimsaidia kufanya hivyo. [4] Kwa hiyo watu
wengi wakakusanyika na kuyazuia maji ya chemichemi zote na mikondo yote
amabayo ilikuwa inatiririka katikati ya nchi. wakasema, “Kwa nini mfalme wa
Ashuru aje na kupata maji mengi?” [5] Hezekia akijipa ujasiri na kuujeenga ukuta wote
uliokuwa umeangushwa chini. Akaijenga minara mirefu, na pia ukuta mwingine
nje. Pia akaiimarisha Milo katika mji wa Dudi, na akafanya kiasi kikubwa cha
silaha na ngao. (Maanshi ya kale yanasema hivi: “ Badala ya, “akajenga minara
amirefu”, baadhi ya matoleo ya zamani na kisasa yanasema, “akajenga minara
mirefu juu yake”, Hii ni juu ya ukuta). [6] Akaweka maamri jeshi juu wa watu.
Akawakusanya pamoja kwake katika sehemu pana kwenye lango la mji na akasema
kwao kwa ujasiri. Akasema, [7] “Muwe imara na wenye ujasiri mzuri. Msiogope
wala kukata tamaa kwa sababu ya mfalme wa Ashuru na jeshi lote ambalo liko
naye, kwa maana kuna mtu yuko pamoja nasi ambaye ni mkuu kuliko [8] walio naye
mfalme wa Ashuru. walionaye ni jeshi la mwili tu, lakini aliye nasi ni Yahwe, Mungu
wetu, kwa ajili ya kutusaidia, na kupiagana vita vyetu.” Kisha watu wakajifariji
wenyewe kwa maneno ya Hezekia, mfalme wa Yuda. [9] Baada ya hayo, Senakeribu,
mfalme wa Ashuru, aliwatuma watumishi wake kwenda Yetusalemu (sasa alikuwa
mbe ya Lakishi, na jeshi lake lote lilikuwa pamoja naye), kwa Hezekia, mfaalme
wa Yuda, na watu wote wa Yuda walikuwa Yerusalemu. Akasema, [10] “Hivi ndivyo
Senakeribu, mfalme wa Ashuru, anasema: Ni kitu gani mnategemea kwa ajili ya
kuhimili uvamizi katika Yerusalemu? [11] Je, Hezekia hawapotoshi ninyi, ili kwamba
awatoe kufa kwa njaa na kiu, anapowaambia, “Yahwe Mungu wetu atatuokoa na
mkono wa mfalme wa Ashuru? [12] Je, siyo Hezekia yule yule ambaye amezipeleka
juu sehemu zake na madhabahu zake na kuwaamuru Yuda na Yerusalemu, juu
ya madhabahu moja lazima muabudu, na juu yake lazima mchome sadaka zenu?
[13] Je, hamjui mimi na babu zangu tulifanya nini kwa makundi ya wote wa inchi
zingine? Je, miungu ya watu wa hizo nchi iliweza kwa njia yoyote kuziokoa nchi

zao zidi ya nguvu zangu? [14] Miongoni mwa miungu yote ya mataifa hayo amabayo
babu zangu waliwatekeza, je, kulikuwa na muungu yeyote aliyeweza kuwaokoa watu
wake kutoka kwenye mkono wangu? Itakuwaje Mungu wenu aweze kuwakoa ninyi
zidi ya nguvu zangu? [15] Sasa msimuruhusu Hezekia awadanganye au kuwashawishi
katika njia hii. Msimwamini, kwa maana hakuna muungu wa taifa lolote au ufalme
amewahi kuwaokoa watu wake nje ya mkono wangu, au nje ya mkono wa babu
zangu. Sembuse na Mungu wenu kwa namna gani atawaokoa na mkono wangu?
[16] Watumishi wa Senakeribu hata walinena mabaya zaidi juu ya Yahwe Mungu na
juu ya mtumishi wake Hezekia. [17] Senakeribu pia akandika barua ili kumdhihaki
Yahwe, Mungu wa Israeli, na kunena kinyume naye. Alisema, “Kama ambavyo
miungu ya mataifa haikuwaokoa watu wake kutoka kwenye mkono wangu, hivyo
hivyo na Mungu wa Hezekia hatawaokoa watu wake kutoka kwenye mkono wangu.”
[18] Wakawalilia kwa lugha ya Wayahudi watu wa Yerusalemu waliokuwa juu ya ukuta,
ili kuwaogopesha na kuwasumbua, ili kwamba waweze kuuteka mji. [19] Wakamnenea
Mungu wa Yerusalemu kama walivyowanenea miungu wa Dunia, ambao ni kazi ya
mikono ya wanadamu tu. [20] Hezekia, mfalme, na Isaya mwana wa Amozi, nabii,
wakaomba kwa sababu ya jambo hili na wakalia hadi mbinguni. [21] Yahwe akatuma
malaika, ambaye aliwaua wanaume wa kupigana vita, majemedari, na maakida wa
mfalme katika kambi. Kwa hiyo Senakeribu akarudi katika nchi yake akiwa na uso
wa aibu. Alipokuwa ameenda katika nyumba ya muungu wake, baadhi ya watoto
wake wakamuua huko kwa upanga. [22] Katika namna hii, Yahwe akamwokoa Hezekia
na wakazi wa Yerusalemu kutoka kwenye mkono wa Senakeribu, mfalme wa Ashuru,
na kutoka kwenye mikono ya wengine, na akawapa pumzika juu ya kila upande.
(Maandishi ya kale yanasema hivi: badala ya “akawapa pumziko juu ya kila pande”,
baadhi ya matoleo ya zamani na ya kisasa yanasema, “akawaongoza juu ya kila
pande”). [23] Wengi walikuwa wakileta sadaka kwa Yahwe katika Yarusalemu, na
zawadi za thamani kwa Hezekia mfalme wa Yuda, kwa hiyo aliinuliwa mbele za
macho ya mataifa yote toka wakati huo na kuendelea. [24] Katika siku hizo Hezekia
akaugua hadi hatua ya kufa. Akaomba kwa Yahwe, ambaye alisema kwake na
kumpa ishara kwamba angeponywa. [25] Lakini Hezekia hakumlipa Yahwe kwa ajili
ya msaada uliotolewa kwake, kwa maana moyo wake uliinuliwa juu. [26] Kwa hiyo
hasira ikaja juu yake, na juu ya Yuda na Yerusalemu. Hata hivyo, baadaye Hezekia
alijinyenyekesha mwenyewe kwa jali ya kiburi cha moyo wake, wote Yeye na wakaaji
wa Yerusalemu, hivyo hasira ya Yahwe haikuja juu yao wakati wa siku za Hezekia.
[27] Hezekia alikuwa na utajiri mwingi sana na heshima kubwa. Alijipatia mwenyewe
vyumba vya kuhifadhia kwa ajili ya fedha, dhahabu, vito vya thamani, na kwa ajili
ya manukato, na kwa ajili ya ngao na na vyombo vyote vya thamani pia. [28] Pia
alikuwa na nyumba za maghala kwa ajili ya mavuno ya nafaka, divai mpya, na
mafuta, na malisho kwa ajili ya aina zote za wanyama. [29] Pia alikuwa na makundi
katika mazizi. Zaidi ya hayo, alijipatia mwenyewe miji na makundi ya na ng'ombe
kwa wingi, kwa maana Mungu alaikuwa amempa afya tele. (Maandishi ya kale
yanasema hivi: Badala ya “miji” baadji ya matoleo ya kisasa yanasema “punda”, na
baadhi mengine ya kisasa yanaacaha neno nzima) [30] Alikuwa ni Hezekia huyu huyu
ambaye alisimamisha chemi chemi ya juu ya maji ya Gihoni, na aliye ileta moja kwa
moja chini upande wa magharibi mwa mji wa Daudi. Hezekia alifanikiwa katika
miradi yake yote. [31] Hata hivyo, katika jambo la mabolozi wa wakuu wa Babeli,
waliotumwa kwake kuwauliza waliofahamu, kuhusu ishara za miujiza iliyokuwa
imefanywa katika nchi, Mungu alimwachia mwenyewe, ili kumjaribu, na kujua yote
yaliyokuwa katika moyo wake. [32] Kwa mambo mengine kuhusu Hezekia, pamoja na
matendo yake ya uaminifu wa agano, unaweza kuona kwamba yameandikwa katika

Maono ya Nabii Isaya Mwana wa Amozi, na katika kitabu cha wafalme wa Yuda na
Israeli. 33 Hezekia akalala pamaoja na babu zake, na wakamzika katika mlima wa
makaburi ya vizazi vya Daudi. Yuda wote na wakaaji wa Yerusalemu wakamheshimu
katika kifo chake. Manase mwanaye akawa mfalme katika nafasi yake.

# 33

1 Manase alikuwa na umri wa miaka kumi na mbili alipoanza kutawala, alitawala
miaka hamsini na tano katika Yerusalemu. 2 Akafanya yalikuwa uovu katika macho
ya Yahwe, kama yalivyo mambo ya machukizo ya mataifa ambao Yahwe alikuwa
amewafukuza mbele ya watu wa Israeli. 3 Kwa maana alizijenga tena sehemu za
juu ambazo baba yake Hezekia alikuwa amezibomoa, na akajenga madhabahu kwa
ajili ya mabaali, akatengeneza sanaamu za Maashera, na akaziinamia chini nyota
zote za mbinguni na kuziabudu. 4 Manase akajenga madhbahu za kipagani katika
nyumba ya Yahwe, ingawa Yahwe alikuwa amemwamuru, “Ni katika Yerusalemu
ambamo jina langu litawekwa milele”. 5 Alijenga madhabahu kwa ajili ya nyota
zote za mbinguni katika vile viwanja viwili vya nyumba ya Yahwe. 6 Katika bonde
la Beni Hinomu akawaweka wanaye katika moto. Akafanya misemo ya ubashiri,
na uchawi, akassoma utabiri; akashauriana na wale waliozungumza na wafu na
wale waliozungumza na na roho. Akafanaya maaovu mengi katika mcho ya Yahwe
na alimfanya Mungu akasirike. 7 Ile sanamu ya Maashera aliyokuwa amefanya,
akaipeleka katika nyumba ya Mungu. Ni kuhusu nyumba hii ambayo Mungu alikuwa
amesema kwa Daudi na Selemani mwanaye; alikuwa amesema, “Ni katika nyumba
hii na katika Yerusalemu, ambao nimeuchangua kutoka makabila yote ya Israeli,
kwamba nitaliweka jina langu milele. 8 Sitawaondoa tena watu wa Israeli katina
nchi hii ambayo niliitoa kwa babu zao, ikiwa tu watakuwa makini katika kuyashika
yote niliyowaamuru, kuzishika sheria zangu, amri zangu, na sheria zangu nilizowapa
kupitia Musa.” 9 Manase akawaongoza Yuda na wakaaji wa Yerusalemu hata kufanya
uovu zaidi kuliko hata watu wa mataifa ambao Yahwe alikuwa amewateketeza
mbele za Israeli. 10 Yahwe akasema kwa Manase, na kwa watu wake wote, lakini
hawakumsikiliza. 11 Kwa hiyo Yahwe akaleta juu yao maamri jeshsi wa jeshi la
Ashuru, ambao walimchukua Manase katika minyonyoro, wakamfunga kwa pingu,
na wakampeleka Babeli. 12 Manase alipokuwa katika dhika, alimuomba Yahwe,
Mungu wake, na akajinyenyekesha sana mbele za Mungu wa babu zake. 13 Akaomba
kwake; na Mungu akamsikiliza, na Mungu akasikia kuomba kwake na akamrudisha
Yerusalemu, katika ufalme wake. Kisha Manase akafahamu kwamba Yahwe alikuwa
Mungu. 14 Baada ya hayo, manase akajenga ukuta wa nje ya mji wa Daudi, upande wa
magharibi wa Gihoni, katika bonde, hadi kwenye lango la Samaki. Akauzungushia
mlima wa Ofeli na akaupandisha ukuta hadi usawa mrefu sana. Akaweka maamri
jeshi jasiri katika ngome zote za miji ya Yuda. 15 Akaipeleka mbali miungu yote
ya kigeni, akaondoa sanamu zote kwenye nyumba ya Yahwe, na madhabahu zote
ambazo alikuwa amejenga juu ya mlima wa nyumba ya Yahwe na katika Yerusalemu,
na kuvitupa nje ya mji. 16 Akaijenga tena madhabahu ya Yahwe na juu yake akatoa
sadaka za amani na sadaka za shukrani; akamwamuru Yuda amtumikie Yahwe,
Mungu wa Israeli. 17 Hata hivyo watu bado walitoa sadaka mahali pa sehemu
za juu, lakini kwa Yahwe, Mungu wao pekee. 18 Katika mambo mengine kuhusu
Manase, maombi yake kwa Mungu wake, na maneno ya waonaji ambao walisema
kwake katika jina la Yahwe, Mungu wa Israeli, tazama, yameandikwa miongoni mwa
matendo ya wafalme wa Israeli. 19 Katika matukio hayo kuna historia ya maombi
yake, na jinsi Mungu alivyoguswa na maomabi hayo. Pia kuna kumbu kumbu ya
dhambi zake zote na makosa yake, na sehemu ambako alikuwa amejenga sehemu za

juu na kuzisimamisha Maashera na sanamu za kuchonga, kambla ya kujinyenyekesha
mwenyewe — na imeandikwa kuhusu hayo katika tarehe ya waonaji. (Maandishi
ya kale yanasema hivi, "tarehe ya Hozai," ambayo ni maandishi ya kifungu asili.
Lakini matoleo mengi ya kisasa yamesahihisha na kusomeka "tarehe ya waonaj"
Pia, matoleo machache ya kisasa yanasema "tarehe ya waonaji".). [20] Kwa hiyo
Manase akalala na babu zake, na wakamzika katika nyumba yake mwenyewe.
Amoni, mwaye, akawa mfalme katika nafasi yake. [21] Amoni alikuwa na umri
wa miaka ishirini na mbili alipoanza kutawala; alitawala miaka miwili katika
Yerusalemu. [22] Akafanya yaliyokuwa uovu katika macho ya Yaahwe, kama Manase,
baba yake, alivyofanya. Amoni alitoa sadaka katika sanamau zote za kuchonga
ambazo alitengeneza Manase baba yake, na aliziabudu. [23] Hakujinyenyekesha mbele
za Yahwe, kama baba yake Manase alivyokuwa amefanya. Badala yake, Amoni
huyu huyu alifanya makosa zaidi na zaidi. [24] Watumishi wake wakapanga njama
wa zidi yake na wakamua katika nyumba yake mwenyewe. [25] Lakini watu wa nchi
wakawaua wote waliofanya njama zidi ya Mfalme Amoni, na wakamfanya Yosia,
mwanaye, mfalme katika nafasi yake.

# 34

[1] Yosia alikuwa na umri wa miaka kumi na nane alipoanza kutawala; alitawala
miaka thelathini na moja katika Yerusalemu. [2] Alifanya yaliyohaki katika macho
ya Yahwe, na alitembea katiaka njia za Daudi babu yake, ha hakugeuka mbali
iwe kulia au kushoto. [3] Kwa maana ndani ya miaka minane ya ya utawala wake,
alipokuwa bado kijana, alianza kumtafuta Mungu wa Daudi, babu yake. Katika
miaka ishirini, alianza kuisafisha Yuda na Yerusalemu kutoka sehemu za juu, vituo
vya Maashera, na sanamu za kuchonga na sanamu za chuma ya kuyeyushwa.
[4] Watu wakazivunja madhabahu za Baali katika uwepo wake; akazibomoa nguzo
za Maashera na na zile sanamu za kuchonga, na sanamu za chuma ya kuyeyushwa
katika vipande hadi zikawa mavumbi. Akayasamabaza mavumbi juu ya makaburi
ya wale ambao walizitolea sadaka. [5] Akaichoma mifupa ya makuhani wao juu ya
madhabahu zao. Katika namna hii, akaisafisha Yuda na Yerusalemu. [6] Alifanya
hivyo hivyo katika miji ya Manase, Efraimu, na Simeoni, sehemu zote hadi Neftali,
na katika maeneo yaliyoizunguka. [7] Alizivunja madhabahu, akayapiga Maashera, na
sanamu za kuchonga kuwa unga, na kuzisambaratisha madhabahu zote za uvumba
katika nchi yote ya Israeli; kisha akarudi Yerusalemu. [8] Sasa katika kipindi cha
miaka ishirini ya utawala wake, baada ya Yosia kuisafisha nchi na hekalu, alimtuma
Shafani mwana wa Azali, Manaseya, akida wa mji, na Yoa mwana wa Yoahazi
katibu, kuikarabati nyumba ya Yahwe Mungu wake. [9] Wakaenda kwa Hilkia, kuhani
mkuu, na wakakabidhi kwake fedha ambazo zilikuwa zimeletwa kwenye nyumbaa
ya Mungu, ambazo Walawi, walinzi wa milingo, walikuwa wamekusanya kutoka
Manase na Efraimu, kutoka kwa masalia wote wa Israeli, kutoka Yuda yote na
Benyamini, na kutoka kwa wakaaji wa Yerusalemu. [10] Wakaikabidhi ile fedha kwa
watu waliosimamia kazi ya hekalu la Yahwe. Watu wale wakawalipa wafanya kazi
walioilikarabati na kulijenga tena hekalu. [11] Wakawalipa maseremala na wajenzi
kwa ajili ya kununulia mawe ya kuchonga na mbao kwa ajili ya kuungia, na
kutengeneza boriti za nyumba amabazo baadha ya wafalme wa Yuda waliziacha
zikachakaa. [12] Watu waliifanya kazi kwa uaminifu. Wasimamizi wao Yahathi
na Obadia, Walawi, wa wana wa Merari; na Zekaria na Meshulamu, kutoka kwa
wana wa Wakohathi. Walawi wengine, wote kati ya wale waliokuwa wanamziki
wazuri sana, kwa ukaribu waliwaelekeza watendakazi. [13] Walawi hawa walikuwa
viongoziz wa wale waliobeba vifaa vya ujenzi na watu wengine wote waliofanya

kazi kwa namna yoyote ile. Pia palikuwa na Walawi ambao walikuwa makatibu,
watawala na walinda lango. 14 Walipoileta fedha ambayo ilikuwa imeletwa kwenye
nyumba ya Yahwe, Hilkia yule kuhani akakiokota kitabu cha sheri ya Yahwe
ambacho kilikuwa kimetolewa kupitia Musa. 15 Hilkia akamwambia Shafani yule
mwandishi, "Nimekiokota kitabu cha sheria katika nyumba ya Yahwe". Hilikia
akakileta kitabu kwa Shefani. 16 Shefani akakipelek kitabu kwa mfalme, na pia akatoa
taarifa kwake, akisema, "Watumishi wako wanafanya kila kitu walichokabidhiwa.
17 Waliitoa feedha yote amabayo ilionekana katika nyumba ya Yahwe, na waliikabidhi
katika mikono ya wasimamizi na watendakazi." 18 Shefani mwandishi akamwambia
mfalme." Hilkia kuhani amenipa kitabu." Kisha Shefani akamsomea mfalme katika
hicho kitabu. 19 Ikawa kwamba mfalme alipokuwa ameyasikia maneno ya sheria,
aliyararua mavazi yake. 20 Mflme akawaamuru Hilkia, Ahikamu mwana wa Shafani,
Abdoni mwana wa Mika, Shafani mwaandishi, na Asaya, mtumishi wake, akisema,
21 "Nendeni mkaulize mapenzi ya Yahwe kwa ajili yangu, na kwa wale waliobaki
katika Israeli na Yuda, kwa sababu ya maneno ya kitabu ambacho kimeokotwa.
Kwa maani ni kikuu, kwa sababu babu zetu hawakuyasikiliza maneno ya kitabu
hiki ili kuyatii yote yaliyokuwa yameandikwa ndani yake". (Badala ya "ambayo
yamemiminwa juu yetu", baadhi ya matoleo yanasema " ambayo yamemulikwa
zidi yetu"). 22 Kwa hiyo Hilkia, na wale ambao mfalme alikuwa amewaamuru,
wakaenda kwa Hulda nabii wa kike, mke wa Shalumu mwana wa Tohathi mwana
wa Hasra, mtunza mavazi (aliishi katika Yerusalemu katika wilaya ya pili), na
walizungumza naye katika namna hii. 23 Akasema kwao, "Hivi ndivyo Yahwe, Mungu
wa Israeli, anasema: Mwambie mtu aliyewatuma kwangu, 24 Hivi ndivyo Yahwe
anasema: Ona, niko karibu kuleta maafa juu ya sehemu hii na wakaaaji wake,
laana zote zilizoandikwa katika kitabu walichokisoma mbele ya mfalme wa Yuda.
25 Kwa sababu wamenisahau na wametoa sadaka za uvumba kwa miungu mingine,
ili kwamba waniweke katika hasira kwa matendo yote waliyofanya — kwa hiyo
hasira yangu itamiminwa juu ya hii sehemu, na haitazimishwa. (Badala ya "ambayo
yamemiminwa juu yetu", baadhi ya matoleo yana "amabyo yamemlikwa zidi yetu".)
26 Lakini kwa mfalme wa Yuda, aliyewatuma kumuuliza Yahwe alichopaswa kufanya,
hivi ndivyo mtakavyosema kwake, 'Yahwe, Mungu wa Israeli anasema hivi: Kuhusu
maneno uliyosika, 27 kwa sababu moyo wako ulipondeka, na ulijinyenyekeza mbele
yangu ulipoyasikia maneno yake zidi ya sehemu hii na wakaaji wake, na kwa sababu
umejinyenyekeza mwenyewe mbele zangu, pia nimekusikiliza —hili ni azimio la
Yahwe— 28 ona, nitakukusanya kwa mababu zako. Utakusanywa katika kaburi lako
kwa amani, na macho yako hayataona maafa yoyoye nitakayoleta juu ya sehemu hii
na wakaaji wake". Wale watu wakarudisha ujumbe huu kwa mfalme. 29 Mfalme
akatuma wajumbe na kuwakusanya wazee wote wa Yuda na Yerusalemu. 30 Kisha
mfalme akaenda kwenye nyumba ya Yahwe, na watu wote wa Yuda wakaaji wa
Yerusalemu, na makuhani, Walawi, na watu wote, kuanzia wakubwa hadi wadogo.
Kisha akasoma mbele zao maneno yote ya kitabu cha Agano kilichokuwa kimeokotwa
katika nyumba ya Yahwe. 31 Mfalme aksimama katika sehemu yake na kufanya
aganao mbele za Yahwe, kutembea mbele za Yahwe, na kuzishika amri zake, taratibu
zake, na sheria zake, kwa moyo wake wote na roho yake yote, kuyatii maneno
ya agano yaliyokuwa yameandikwa katika agano ambayo yalikuwa yameandikwa
katika kitabu hiki. 32 Aliwasababisha wote walioonekana katika Yerusalemu na
Benyamini kusimama kwa agano. Wakaaji wa Yerusalemu wakatembea kwa agano
la Mungu, Mungu wa babu zao. 33 Yosia akapeleka mbali mambo yote ya machukizo
kutoka kwenye nchi iliyomilikiw na watu wa Israeli. Akamfanya kila mtu katika
Israeli amwabudu Yahwe, Mungu wao. Kwa maisha siku zake zote, hawakugeka

mbali kwa kutomfuata Yahwe, Mungu wa mababu zao.

# 35

1 Yosia asherehekea Pasaka kwa ajili ya Yahwe katika Yerusalemu, na wakachinja
wanakondoo katika siku ya kumi na nne ya mwezi wa kwanza. 2 Akawaweka
makauhuni katika nafasi zao na akawatia moyo katika hudumza za nyumba ya
Yahwe. 3 Akasema kwa Walawi waliowafundisha Israeli wote na waliokuwa
wamewekwa wakifu kwa Yahwe. "Liwekeni sanduka takatifu katika nyumba ambayo
Selemani mwana wa Daudi, mfalme wa Israeli aliijenga. Msilibebe kuzunguka nalo
tena mabegani mwenu. Sasa mwabuduni Yahwe Mungu wenu, na watumikieni watu
wake Israeli. 4 Jikusanyeni wenyewe kwa majina ya nyumba za babu zenu na zamu
zenu, mkifuata maelekezo ya Daudi, mfalme wa Israeli, na yale ya Selemani, mwaye.
5 Simeni katika sehemu takatifu, mkichukua nafasi zenu kwa zamu zenu ndani ya
nyumba za mababu wa bdugu zenu, uzao wa watu, na mchukue sehemu zenu kwa
zamu zenu ndani ya nyumba za mababu wa Walawi. 6 Chinjeni wanakondoo wa
Paska, jitakaseni wenyewe, andaeni wankondoo kwa ajili ya ndugu zenu, kufanya
sawa sawa na neno la Yahwe ambalo lilitolewa kwa mkono wa Musa". 7 Yosia
akawapa watu wote wanakondoo elfu thelathini na wanambuzi kutoka katika
makundi kwa ajili ya sadaka za Pasaka kwa wote walikuwepo. Pia akatoa ng'ombe
dume elfu tatu; hawa walikuwa kutoka katika mali ya mfalame. 8 Viongozi wake
wakatoa sadaka za hiari kwa watu, makuhani, na Walawi. Hilki, Zekaria, na Yeieli,
viongozi wasimamizi wa nyumba ya Mungu, wakawapa makuhani ndama 2, 600
na maksai mia tatu kwa ajili ya matoleo ya Paska. 9 Pia Konania, Shemaya na
Nethaneli, ndugu zake, na Hashabia, Yeieli, na Yazabadi, mkuu wa Walawi, akawapa
Walawi ndama elfu tano kwa ajili ya matoleo ya Pasaka. 10 Kwa hiyo huduma
iliandaliwa, na makuhani wakasimama katika sehemu zao, pamoja na Walawi kwa
zamu zao, kwa mjibu wa agizo la mfalme. 11 Wakawachinja wanakondoo wa Pasaka,
na makuhani wakainyunyiza damu waliyoipokea kutoka kwenye mikono ya Walawi,
na Walawi wakawachuna wanakondoo. 12 Wakaziondoa sadaka za kuteketezwa,
ili kuzisambaza katika makundi ya nyumba za mababu wa watu, ili wamtolee
Yahwe, kama ilivyoandikwa katika Kitabu cha Musa. Wakafanya vile vile kwa
wale ng'ombe dume. 13 Wakawaoka kwa moto wanakondoo wa Pasaka wakifuata
maelekezo, kuhusu sadaka takatifu, walizichemsha kwenye vyungu, masufuria na
makaangoni, na haraka wayapeleka kwa watu. 14 Baadaye waliandaa sadaka kwa
ajili yao wenyewe na kwa ajili ya makuhani, kwa sababu makuhani, uzao wa Haruni,
walikuwa wametingwa katika kazi ya kutoa sadaka za kuteketezwa na za mafuta
hadi usiku ulipoingia, kwa hiyo Walawi wakaandaa sadaka kwa ajili yao wenyewe
na kwa ajili ya makuhani, wana wa Haruni. 15 Waimbaji, wana wa Asafu, walikuwa
katika nafasi zao, kama ilivyoagiwa na Daudi, Asafu, Hemani, na Yeduthuni, mwonaji
wa mfalme, na walinzi walikuwa katika kila lango. Hawakutakiwa kuviacha vituo
vyao, kwa sababu ndugu zao Walawi walifanya maandalizi kwa ajili yao. 16 Kwa
hiyo, wakati huo huduma yote ya Yahwe ilifanyika kwa ajili ya kusherekea Pasaka
na kutoa sadaka za kuteketezwa juu ya madhabahu ya Yahwe, Kama alivyoamuru
mfalme Yosia. 17 Watu wa Israeli ambao walikuwepo wakaishika Sabato wakati
huo, na kisha Sikukuu ya Mikate isiyochachwa kwa siku saba. 18 Pasika kama hiyo
haijafanyika tena katika Israeli tangu siku za nabii Samweli, wala hakuna mfalme
yeyote miongoni mwa wafalme wa Israeli ambaye amewahi kusherekea Pasaka kama
Yosia alivyofanya, pamoja na makuhani, Walawi, na watu wote wa Yuda na Israeli
waliokuwepo, na wakaaji wote wa Yerusalemu. 19 Pasaka hii ilitunzwa ndani ya
miaka kumi na nane ya utawala wa Yosia. 20 Baada ya haya yote, baada ya Yosia
kuliweka hekalu katika utaratibu, Neko, mfalme wa Misiri, akaenda juu kupigana

dhidi ya Karkemist karibu na mto Frati, na Yosia akaenda kupigana juu yake. 21 Lakini
Niko akatuma wajumbe kwake, akisema, "Nikufanye nini, mfalme wa Yuda? Leo
siji kinyume nawe, lakini dhidi ya nyumba ambayo nafanya vita nayo. Mungu
ameniamuru kuwahi, hivyo acha kumwingilia Mungu, ambaye yuko pamoja nami,
la sivyo atakuangamiza." 22 Hata hivyo, Yosia alipuuzia kurudi nyuma. Akajibadili ili
apigane naye. Hakusikiliza maneno ya Neko ambayo yalikuja kutoka kwenye kinywa
cha Mungu; hivyo akaenda kupigana kataika bonde la Megido. 23 Wapiga upinde
wakampiga Mfalme Yosia, na mfalme akawaambia watumishi wake, "Niondoeni
hapa, kwa maana nimejeruhiwa vibaya." 24 Kwa hiyo watumishi wake wakamtoa
nje ya gari, na kumuweka katika gari lake la tahadhari. Wakampeleka Yerusalemu,
ambako alikufa. Alzikwa katika makaburi ya babu zake. Yuda wote na Yerusalemu
wakamwomboleza. 25 Yeremia akamwomboleza Yosia; waimbaji wote wa kiume
na wa kike wakaomboleza kuhusu Yosia hata leo. Nyimbo hizi zikawa desturi
katika Israeli; tazama, zimeandikwa katika nyimbo za maombolezo. 26 Kwa mambao
mengine kuhusu Yosia, na matendo yake mema aliyoyafanya katika utii kwa kile
kilichoandikwa katika sheria ya Yahwe— 27 na matendo yake, kutoka mwanzo hadi
mwisho, yameandikwa katika kitabu cha wafalme wa Yuda na Israeli.

# 36

1 Kisha watu wa nchi wakamchukua Yehoazi mwana wa Yosia, na wakamfanya
mfalme katika nafasi ya baba yake katika Yerusalemu. 2 Yehoazi alikuwa na umri
wa miaka ishirini alipoanza kutawala, na akatawala miezi mitatu katita Yerusalemu.
3 Mfalme wa Misiri akamwondoa katika Yerusalemu, na akaitoza nchi faini ya talanta
za fedha mia moja na talanta moja ya dhahabu. 4 Mfalme wa Misiri akamfanya
Eliakimu, ndugu yake, mfalme juu ya Yuda na Yerusalemu, na akambadili jina lake
kuwa Yehoakimu. Kisha akamchukua ndugu yake Eliakimu - Yeahazi na kumpeleka
Misiri. 5 Yehoakimu alikuwa na umri wa miaka ishini na tano alipoanza kutawala,
na akatawala miaka kumi na moja katika Yerusalemu. Akafanya ambayao yalikuwa
uovu katika macho ya Yahwe Mungu wake. 6 Kisha Nebukadreza, mfalme wa
Babeli, akamvamia na kumfunga katika minyororo kumuongoza kwenda mbali
Babeli. 7 Nebukadreza pia akabeba baadhi ya vitu katika nyumba ya Yahwe kwenda
Babeli, na akaviweka katika ikulu yake huko Babeli. 8 Kwa mambo mengine kuhusu
Yehoyakimu, mambo mabaya aliyofanya, na yaliyopatikana zidi yake, tazama,
yameandikwa katika kitabu cha wafalme wa Yuda na Israeli. Basi Yehoyakimu,
mwanaye, akawa mfalme katika nafasi yake. 9 Yehoyakimu alikuwa na umri wa
miaka minane alipoanza kutawala; alitawala miezi mitatu na siku kumi katika
Yerusalemu. Akafanya yaliyokuwa maovu katika macho ya Yahwe. 10 Katika kipindi
cha mwisho wa mwaka, mfalme Nebukadreza akatuma watu na wakampelekea
Babeli, vitu vya thamani kutoka katika anyumba ya Yahwe, na kumfanya Sedekia
ndugu yake, mfalame juu ya Yuda na Yerusalemu. 11 Sedekia alikuwa na umri
wa miaka isshirini na moja alipoanza kutawala; akatawala miaka kumi na moja
katika Yerusalemu. Akafanya yaliokuwa uovu katika macho ya Yahwe Mungu wake.
12 Hakujinyenyekesha mwenyewe mbele za Yeremia nabii, ambaye alisema kutoka
kwenye kinywa cha Yahwe. 13 Sedekia pia akaasi zidi ya Mfalme Nebukadreza,
ambaye alikuwa amemfanya aape uaminifu kwake kupitia Mungu. Lakini Sedekia
aliishupaza shingo yake na kuufanya moyo wake mgumu usigeuke kwa Yahwe,
Mungu wa Israeli. 14 Vilevile, viongozi wote wa makauhanai na wa watu hawakuwa
waaminifu, na waliufuata uovu wa mataiafa. Waliigoshi nyumba ya Yahwe ambayo
alikuwa ameitakasa katika Yerusalemu. 15 Yahwe, Mungu wa babu zao, akatuma
maneno kwao tena na tena kupitia wajumbe wake, kwa sababu alikuwa na huruma

juu ya watu wake na juu ya sehemu anayoishi. [16] Lakini waliwadhihaki wajumbe wa
Mungu, wakayadharau maneno yake, na kuwackeka manabii wake, hadi hasira ya
Yahwe ilipoinuka zidi ya watu wake, hadi pailipokosekana msaada. [17] Hivyo Mungu
alimpeleka juu yao mfalme wa Wakaldayo, ambaye aliwaua vijana wao kwa upanga
ndani ya patakatifu, na hakuwa na huruma juu ya vijana au mabikra, watu wazee au
wenye mvi. Mungu akawatoa wote mikononi mwake. [18] Vyombo vyote vya nyumba
ya Mungu, vikubwa na vidogo, hazina za nyumba ya Yahwe, na hazina za mfalme
na watumishi wake—vyote hivi akavipeleka Babeli. [19] Wakaichoma moto nyumba
ya Mungu, wakauangusha chini ukuta wa Yerusalemu, wakachoma ikulu zake zote,
na wakaharibu vitu vizuri vyote ndani yake. [20] Mfalme akawapeleka mbali Babeli
wale waliokuwa wameoka na upanga. Wakawa watumishi kwa ajili yake na wanawe
hadi utawala wa Waajemi. [21] Hili lilitokea ili kulitimiza neno la Yahwe kwa kinywa
cha Yeremia, hadi nchi itakapokuwa imefurahia mapumziko ya Sabato yake. Iliishika
Sabato kwa muda mrefu hadi kukataliwa kwake, ili miaka sabini itimie katika namna
hii. [22] Sasa katika mwaka wa kwanza wa Koreshi, mfalme wa Uajemi, ili kwamba
neno la Yahwe kwa kinywa cha Yeremia liweze kutimizwa, Yahwe akaipa hamasa
roho ya Koreshi, mfalme wa Uajemi, kwamba akafanya tangazo katika uflme wake
wote, na akaliweka pia katika maandishi. Akasema, [23] "Hivi ndivyo Koreshi, mfalme
wa Uajemi, anasema: Yahwe, Mungu wa mbinguni, amenipa falme zote za dunia.
Ameniagiza nijenge nyumbaa kwa ajili yake katika Yerusalemu, ambao upo Yuda.
Yeyote aliyemiongoni mwenu kutoma katika watu wake wote, Yahwe Mungu wenu,
awe naye. Aende kwenye ile nchi."

# Ezra

1 Katika mwaka wa kwanza wa Koreshi, mfalme wa Uajemi, Yahwe akatimiza
neno lake ambalo Yeremia alisema, na kuinua roho ya Koreshi. Sauti ya Koreshi
ikasambaa na kusikika katika ufalme wake. Hiki ndicho kilichoandikwa na kusemwa:
2 "Koreshi, mfalme wa Uajemi, anasema: Yahwe, Mungu wa mbinguni, amenipa
mimi ufalme wote wa dunia, na ameniteua mimi kumjengea yeye nyumba katika
Yerusalem ya Yuda. 3 Yeyote katika watu wake (Mungu awe pamoja naye) anaweza
kwenda Yerusalem na kujenga nyumba kwa ajili ya Yahwe, Mungu wa Israel, Mungu
ambaye yuko Yerusalem. 4 Watu wa kila sehemu katika ufalme waliosalia katika nchi
na kuishi wanapaswa kuwapa wao fedha na dhahabu, mali na wanyama, pamoja na
kutoa kwa hiari kwenye nyumba ya Mungu Yerusalem." 5 Ndipo wakuu wa jamii ya
Yuda na Benjamini, makuhani na walawi, na kila mmoja ambaye Roho wa Mungu
alimwinua kuondoka na kujenga nyumba yake alisimama. 6 Wale waliowazunguka
karibu waliwasaidia kwa kuwapa fedha na vitu vya dhahabu, mali, wanyama, vitu
vya thamani, na kutoa kwa hiari. 7 Mfalme Koreshi akarusu vitu ambavyo vilikuwa
kwenye nyumba ya Yahwe, ambavyo Nebukadreza alitoa kutoka Yerusalem na
kuviweka katika nyumba ya miungu yake. 8 Koreshi akavikabidhi kwenye mikono ya
Mithredathi mtunza fedha, ambaye akavitoa na kuhesabu kwa Sheshbaza, kiongozi
wa Yuda 9 Hii ilikuwa idadi yake: beseni thelathini za dhahabu, beseni elfu moja za
fedha, beseni zingine ishirini na tisa, 10 mabakuli thelathini ya dhahabu, mabakuli
madogo ya fedha 410, na vitu elfu moja vya kuongezea. 11 Kulikuwa na vitu 5, 400
vya fedha na dhahabu. Sheshbaza akavileta vyote wakati wa uhamisho kutoka Babeli
kwenda Yerusalem.

## 2

1 Hawa ndio watu katika jimbo waliochukuliwa mateka na kwenda na mfalme
Nebukadneza, yeye aliwachukua utumwani Babeli, watu wakarudi katika miji yao
ya Yerusalem na Yuda. 2 Walikuja pamoja na Zerubabeli, Yoshua, Nehemia, Seraya,
Reelaya, Mordekai, Bilshani, Mispari., Bigwai, Rehumu, na Baana. Hii ndio idadi ya
wanaume ya watu wa Israeli. 3 Waporoshi: 2, 172 4 Wana wa Shefatia: 372 5 Wana
wa Ara: 775. 6 Wana wa Path-Moabu, kupitia Yeshua na Yoabu: 2, 812. 7 Wana
wa Eliamu: 1, 254. 8 Wana wa Zatu: 945. 9 Wana wa Zakai: 760. 10 Wana wa
Binui: 642. 11 Wana wa Bebai: 623. 12 Wana wa Azgadi: 1, 222. 13 Wana wa
Adonikamu: 666. 14 Wana wa Bigwai: 2, 056. 15 Wana wa Adini: 454. 16 Wana
wa Ateri kupitia Hezekiah: tisini na nane. 17 Wana wa Besai: 323. 18 Wana wa
Harifu: 112. 19 Wanaume wa Hashimu: 223. 20 Wanaume wa Gibeoni: Tisini na
tano. 21 Wanaume wa Bethlehemu: 123. 22 Wanaume wa Netofa: Hamsini na sita.
23 Wanaume wa Anathothi: 128. 24 Wanaume wa Beth-Azmawethi: Arobaini na mbili.
25 Wanaume wa Kiriath-Yearimu, na Kefira, na Beerothi: Mia saba arobaini na tatu.
26 Wanaume wa Rama na Geba: 621. 27 Wanaume wa Mikmashi: 122. 28 Wanaume
wa Betheli, na Ai: 223. 29 Wanaume wa Nebo: Hamsini na mbili. 30 Wanaume wa
Magbishi: 156. 31 Wanaume wengine wa Elamu: 1, 254. 32 nne. Wanaume wa Harimu:
320. 33 Wanaume wa Lodi, na Hadidi, na Ono: 725. 34 Wanaume wa Yeriko: 345.
35 Wanaume wa Senaa: 3, 630. 36 Wana wa Yedaya kuhani wa nyumba ya Yoshua:
973. 37 Wana wa Imeri: 1, 052. 38 Wana wa Pashuri: 1, 247. 39 Wana wa Harimu:
1, 017. 40 Walawi: Wana wa Yeshua, na Kadmieli, wana wa Hodavia: Sabini na
41 nne. Waimbaji hekaluni wana wa Asafu: 128. 42 Walinzi: wana wa Shalumu, Ateri
na, Talmoni, Akubu, Hatita na Shobai: 139 jumla. 43 Wale walichaguliwa kuhudumu
ndani ya Hekalu: wana wa Siha, Hasufa, Tabaothi: 44 Keros, Siaha, Padoni. 45 Lebana,

Hagaba, Akubu, 46 Hagabu, Salmai, Hanani 47 Wana wa Gideli, Gahari, Reaya, 48 Resini,
Nekoda, Gazamu, 49 Uza, Pasea, Besai, 50 Asna, Meunimu, Nefusimu: 51 Wana wa
Bakbuki, Hakufa, Harhuri: 52 Basluthi, Mehida, Barsha: 53 Barkosi, Sisera, Tema:
54 Nesia, Tefa 55 Wana wa watumishi wa Selemani: Wana wa Sotai, Soferethi, Peruda,
56 Yaala, Darkoni, Gideli, 57 Shefatia, Hatili, Pokereth-Sebaimu, Amoni, 58 Walikuwa
jumla ya watumishi mia tatu tisini na mbili waliochaguliwa kutumika katika Hekalu
pamoja na wana wa watumishi wa Selemani. 59 Wale ambao walitoka Tel-mela,
Tel-harsha, Kerubu, Adani, na Imeri, Lakini hawakuweza kuthibitisha kizazi chao
kilitoka Israeli- 60 pamoja na mia sita hamsini na mbili wana wa Delaya, Tobia
na Nekoda. 61 Vilevile, kutoka kwa wana wa kuhani: Wana wa Habaya, Hakosi,
Barzilai {ambaye alipata mke kutoka kwa binti ya Barzilai, Mgileadi na akaitwa
kwa jina lao} 62 Walitafuta kumbukumbu ya kizazi chao, lakini haikupatikana, hivyo
wakaondolewa kwenye ukuhani kama wasiosafi. 63 Hivyo kiongozi akawakataza
wasile kitu chochote kitakatifu kilichotakaswa mpaka kuhani mwenye Urimu na
Thumimu athibitishe. 64 Jumla ya kundi 42, 360, 65 ukiondoa watumishi na wasaidizi
(wao walikuwa 7, 337) waimbaji Hekaluni wanaume na wanawake (mia mbili)
66 Farasi wao: 736, Nyumbu wao: 245. 67 Ngamia wao: 435. Punda wao: 6, 720.
68 Walipokwenda kwenye nyumba ya Yahwe Yerusalem, wakuu wa mababa walijitoa
kwa hiari kujenga nyumba. 69 Walitoa kadiri ya uwezo wao katika kufadhili kazi:
Dhahabu za darkoni sitini na moja elfu, mane za fedha elfi tano na mavazi mia moja
ya makuhani. 70 Basi makuhani na walawi, watu, waimbaji hekaluni, na walinzi
wa getini, na wale waliochaguliwa kutumika katika Hekalu walikaa katika miji yao.
Watu wote katika Israel walikuwa katika miji yao.

# 3

1 Ilikuwa miezi saba baaada ya watu wa Israeli kurudi kwenye miji yao, ndipo
walipojikusanya pamoja kama mtu mmoja katika Yerusalem. 2 Yeshua mwana
wa Yosadaki na kaka yake kuhani, na Zerubabeli mwana wa Sheatieli na kaka
yake wakainuka na kujenga madhabahu ya Mungu wa Israeli na kutoa sadaka ya
kuteketezwa kama ilivyoagizwa katika sheria ya Musa, Mtu wa Mungu. 3 Ndipo
wakaanzisha madhabahu juu ya msingi, kwa hofu waliokuwa nayo kwa sababu
ya watu wa nchi/ Wakatoa sadaka ya kuteketezwa kwa Yahwe asubuhi na jioni.
4 Pia vilevile wakaichunguza sikukuu ya vibanda kama ilivyoandikwa na wakatoa
sadaka ya kuteketezwa siku kwa siku kama ilivyoagizwa, kila siku kwa siku yake.
5 Kulikuwa na sadaka ya kila siku ya kuteketezwa na mwezi mara moja na sadaka
za siku ya Yahwe za kudumu, pamoja na sadaka zote za hiari. 6 Walianza kutoa
sadaka za kuteketezwa za Yahwe siku ya kwanza ya mwezi wa saba, ingawa hekalu
lilikuwa halijaanza kujengwa. 7 Hivyo wakatoa fedha kwa wahunzi na fundi wa
mkono, na wakawapa chakula, vinywaji na mafuta kwa watu wa Sidoni na Tiro,
ili kwamba walete miti ya mierezi kupitia baharini kutoka Lebanoni mpaka Yafa,
na kama walivyo ruhusiwa na mfalme Koreshi wa Uajemi. 8 Ndipo mwezi wa
pili katika mwaka wa pili baadae wakaja kwenye nyumba ya Mungu Yerusalem,
Zerubabeli, Yoshua mwana wa Yosadaki, na baadhi ya makuhani na walawi na
wale walikuja kutoka uhamishoni kurudi Yerusalem wakaanza kazi. Wakawachagua
walawi walikuwa na miaka ishirini na zaidi kusimamia kazi ya nyumba ya Yahwe,
9 Yoshua akamsimamisha kijana wake na kaka yake, Kadmiel na watoto wake, na
kizazi cha yuda kusimamia kufanya kazi katika nyumba ya Mungu. Pamoja na
wao kulikuwa na wana wa Henadadi, na uzao wao, na pia jamaa zao walawi.
10 Wajenzi wakasimamisha msingi wa Hekalu la Yahwe, Na hii ikawawezesha
makuhani kusimama na mavazi yao wakiwa na tarumbeta, na walawi wana wa

Asafu, kumtukuza Yahwe kwa matoazi, kama mkono wa mfalme Daudi wa Israel
alivyoagiza. 11 Waliimba kwa kumsifu na kumshukuru Yahwe. “Yeye ni mwema!
Agano lake ni kweli kwa Israel ladumu milele.”Watu wote wakapiga kelele kwa
sauti kuu za shangwe wakimsifu Yahwe kwa sababu misingi ya Hekalu ilikuwa
imekamilika. 12 Lakini wengi wa Makuhani, walawi, wakuu wa kale, na wazeee wa
zamani walioiona nyumba ya kwanza, wakati misingi ilipowekwa wakaishuhudia
kwa macho yao, walilia kwa sauti. Lakiniwengi walipiga kelele kwa sauti za
shangwe na furaha na sauti za kushangaza. 13 Na matokeo yake, watu hawakuweza
kutofautisha sauti za furaha na sauti za shangwe na sauti za watu waliokuwa wanalia,
kwa kuwa watu walikuwa wanalia kwa sauti kuu ya shangwe na sauti ilisikika kutoka
mbali.

# 4

1 Ndipo maadui wa Yuda na Benjamini waliposikia kwamba watu waliokuwa
uhamishoni walikuwa wanajenga Hekalu la Yahwe, Mungu wa Israel. 2 Hivyo
wakamkaribia Zerubabeli na wakuu wa jamii yao. Wakawaambia,: Mturuhusu
tujenge pamoja nanyi, kama ninyi, tunamtafuta mungu wenu, na tumejitoa kwake
tangu siku ambapo, Esar-hadoni, mfalme wa Ashuru alipotuleta mahali hapa.”
3 Lakini Zerubabeli, Yoshua na wakuu wa kale wa jamii wakasema, “sio wewe, lakini
sisi ndio tunaowajibika kujenga nyumba ya Mungu wetu, Sisi ndio tutakaomjengea
Yawe, Mungu wa Israel, kama vile mfalme koreshi mfalme wa Ashuru alivyoagiza.”
4 Hivyo watu wa nchi wakadhoofisha mikono ya wayahudi, wakawafanya wayahudi
waogope kujenga nyumba. 5 Pia wakawahonga washauri ili kuwachanganya katika
mipango yao. Walitenda haya kipindi chote cha Koreshi na kipindi cha utawala
wa Dario mfalme wa Uajemi. 6 Tena katika kuanza kutawala kwake Ahasuero
wakaandika mashitaka dhidi ya wenyeji wa Yuda na Yerusalem 7 Ilikuwa siku za
Ahasuero ambazo Artashasta, Mithredathi, na Tabeeli na wenzake wakamwandikia
Ahasuero. Barua iliandikwa Kiaramu na kutafsiliwa. 8 Rehumu jemedari na Shimshai
mwandishi wakaandika hivi kwa Artashasta kuhusu Yerusalem. 9 Tena Rehumu,
Shimshai na wenzao ambao ni waamuzi na maofisa wengine wa Serikali, kutoka
Waarkewi, Wababeli na washushami katika Waelami, 10 nao wakaandika barua
na waliungana na watu wakuu na mheshimiwa Asur - bani - pali aliwalazimisha
kukaa Samalia pamoja na waliobaki katika mji ngambo ya mto. 11 Hii ni nakala
waliotuma kwa Artashasta: “Watumishi wako, watu wa mji ngambo ya mto,
waandika hivi: 12 Mfalme atambue kwamba Wayahudi waliotoka kwako wamefanya
kinyume chetu hapa Yerusalem wamejenga mji wa uasi. Wamekamilisha ukuta na
marekebisho ya misingi. 13 Sasa mfalme atambue kwamba endapo mji utajengwa
na kuta zake kukamilika, hawatatoa ushuru na kodi, lakini watawadhuru wafalme.
14 Hakika kwa kuwa tumekula chumvi ya Ikulu, haitopendeza sisi kuona heshima
ya mfalme inavunjwa, kwa sababu hiyo tunamtaarifu mfalme 15 kufanya uchunguzi
wa kumbukumbu ya baba yake, na kujiridhisha kuwa mji huu ulikuwa wa uharibifu
ambao utawadhuru wafalme na miji. Ulisababisha matatizo mengi kwa wafalme
na miji. Ilikuwa ni kitovu cha uhalibifu tokea siku nyingi. Ni kwa sababu hiyo
mji uliteketezwa. 16 Tunamtaarifu mfalme kuwa endapo mji na ukuta ukijengwa,
Hakuna kitakachobakia kwa ajili yako katika mji ngambo ya mto.” 17 Ndipo
mfalme akarudisha majibu kwa Rehumu na Shimshai na wenzao katika Samalia
na waliobaki katika mji ngambo ya mto. “Amani iwe pamoja nanyi. 18 Barua
mliyonitumia imetafsiliwa na kusomwa kwangu. 19 Hivyo niliagiza uchunguzi
ufanywe na ikabainika kwamba zamani uliasi na kuwafitinisha wafalme. 20 Wafalme
wakuu walitawala Yerusalem yote na kuongoza kila sehemu ya mji ngambo ya mto.
Ada na kodi walilipwa. 21 Sasa, wekeni agizo kwa watu hawa wasiendelee na kujenga

mji mpaka nitakapotoa amri. 22 Muwe waangalifu msipuuze hili. Kwa nini kuruhusu
tishio hili kuongezeka na kusababisha hasara kwa matakwa ya ufalme? 23 Baada
ya amri ya mfalme Artashasta kusomwa mbele ya Rehumu, Shimshai na wenzao,
wakaondoka haraka kwenda Yerusalem, na wakawalazimisha Wayahudi kuacha
kujenga. 24 Hivyo kazi ya nyumba ya Mungu Yerusalem ikasitishwa mpaka kutawala
mara ya pili kwa mfalme Dario wa Uajemi.

# 5

1 Ndipo Hagai nabii na Zakaria mtoto wa Ido nabii wakatabiri kwa jina la Mungu
wa Israel kwa wayahudi wa Yuda na Yerusalem. 2 Zerubabeli mtoto wa Shealtieli
na Yoshua mtoto wa Yosadaki wakainuka na kuanza kujenga nyumba ya Mungu
Yerusalem pamoja na manabii ambao waliwahamasisha wao. 3 Ndipo Tatenai
Mkuu wa mji ngambo ya mto, Shethar - Bozenai, na mshirika wao, wakaja na
kusema kwao, “Nani aliyewapa agizo la kujenga nyumba hii na kukamilisha ukuta?”
4 Vilevile walisema, “Ni majina ya watu gani wanaoshughulika na ujenzi huu?”
5 Lakini jicho la Mungu lilikuwa pamoja na viongozi wa Wayahudi na maadui wao
hawakuweza kuwazuia. Walikuwa wakisubiri barua kutumwa kwa mfalme na amri
kurudi kwao kwa ajili ya suala hili. 6 Hii ni nakala ya barua kwa Tatenai, mkuu
wa mji ngambo ya mto, na Shethar - Bozenai na wenzao katika mji ngambo ya
Mto, ambao waliwatuma kwa mfalme Dario. 7 Wakatuma ujumbe, wakiandika kwa
mfalme Dario, “Amani tele iwe kwako” 8 Mfalme atambue kwamba tulikwenda Yuda
kwenye nyumba ya Mungu Mkuu. Imeshajengwa kwa mawe makubwa na mbao
zimewekwa katika kuta. Hii kazi inafanyika kwa utaratibu na inaendelea vizuri kwa
mikono yao. 9 Tukawauliza wazee, ni nani aliyewapa agizo la kujenga nyumba na
ukuta?' 10 Pia tuliwauliza majina yao ili kwamba ujue majina ya kila mtu ambaye
aliwaongoza. 11 Nao wakatujibu na kusema, “Sisi tu watumishi wa Mungu wa
mbingu na nchi na sisi tunaijenga nyumba hii ambayo ilijengwa miaka mingi iliyopita
wakati mfalme mkuu wa Israel alijenga na kuikamisha. 12 Ingawa, watangulizi wetu
walipomchukiza Mungu wa mbinguni, Mungu akawatia katika mikono ya mfalme
wa Babeli Nebukadineza, ambaye alivunja nyumba na kuwachukua watu mateka
Babeli. 13 Pia, katika mwaka wa kwanza wa kutawala Koreshi mfalme wa Babeli,
Koreshi aliamuru nyumba ya Mungu kujengwa. 14 Mfalme Koreshi pia alirudisha vitu
vya dhahabu na fedha vya nyumba ya Mungu ambavyo Nebukadineza alivichukua
kwenye hekalu Yerusalem na kuvipeleka kwenye hekalu Babeli. Naye akavitunza
kwa Sheshbaza, ambaye alimchagua kuwa kiongozi. 15 Naye akamwambia, “Chukua
hivi vitu. Uondoke na kuviweka kwenye Hekalu Yerusalem. Na nyumba ya Mungu
ijengwe kule.” 16 Ndipo huyu Sheshbaza akaja na kuweka msingi kwa nyumba ya
Mungu katika Yerusalem: na ikaendelea kujengwa, lakini bado haijakamilika 17 Sasa
ikiwa itampendeza mfalme, na uchunguzi ufanyike kwenye nyumba ya ukumbusho
Babeli Ikiwapo hukumu ya mfalme wa Koreshi ya kujenga nyumba ya Mungu
Yerusalem. Na mfalme anaweza kutuma uamuzi wake kwetu.

# 6

1 Na mfalme dario akaamuru uchunguzi ufanyike katika nyumba ya kumbukumbu
Babeli. 2 Na katika mji wa Akmetha huko media chuo kilionekana: Kumbukumbu
yake ilisema: 3 “Katika mwaka wa kwanza mfalme Koresh, Koreshi alitoa amri
kuhusu nyumba ya Mungu Yerusalem:'Na nyumba ijengwe iwe sehemu ya kutoa
dhabihu, misingi yake iwekwe, urefu wake uwe sitini, 4 na upana wake uwe sitini,
sehemu tatu za mawe makubwa na sehemu moja ya mbao mpya, na gharama hizo
zitalipwa kutoka nyumba ya mfalme. 5 Sasa virudishwe tena vitu vya dhahabu na
fedha vilivyokuwa kwenye nyumba ya Mungu ambavyo Nebukadineza alivichukua

kuvipeleka Babeli kutoka kwenye Hekalu Yerusalem. Na avirudishe tena Yerusalem
Hekaluni. Na utaviweka tena kwenye nyumba ya Mungu. 6 Sasa Tetanai, mkuu
wa jimbo ngambo ya mto, Shethar - Bozenai na wenzao walio katika mji ngambo
ya mto, wakajitenga, 7 wakaacha kazi ya nyumba ya Mungu pekee. Viongozi na
wazee wa kiyahudi watajenga nyumba ya Mungu mahali pake. 8 Ninatoa agizo
kwamba lazima lifanyike kwa wazee wa kiyahudi wanaojenga nyumba ya Mungu:
Mchango kutoka kwa mfalme ushuru ngambo ya mto, utatumika katika kuwalipa
watu hawa ili kwamba kazi yao isiweze kusimama. 9 Chochote kitakachohitajika,
ngombe wachanga, kondoo au kondoo wa sadaka ya kutekezwa kwa ajili ya Mungu
wa mbinguni, ngano, chumvi, divai na mafuta kadri ya maagizo ya makuhani wa
Yerusalem - wapatie vitu hivi kila siku bila kikomo. 10 fanya hivyo ili kwamba
wataleta sadaka kwa Mungu wa mbinguni na wataomba kwa ajili yangu mfalme
na watoto wangu. 11 Mimi nina agiza kwamba yeyote atakayevunja amri hii, Chuma
kitolewe katika nyumba yake. Na awekwe juu yake. Na nyumba yake itabadilishwa
kuwa takataka kwa sababu hii. 12 Mungu huyu aliyesababisha jina lake kuwepo
atamwondoa mfalme au mtu atakayebadili agizo hili au kuondosha nyumba ya
Mungu katika Yerusalem. Mimi Dario nimeagiza hili, lifanyike kwa makini. 13 Na kwa
sababu ya amri iliyotumwa na mfalme Dario, Tatenai kiongozi mji ngambo ya mto na
Sheshthar -Bozenai na wenzao. wakafanya kila kitu kama Mfalme Dario alivyoagiza.
14 Hivyo wazee wa kiyahudi wakajenga kama Hagai na Zakaria walivyoelekeza kwa
kutabiri. Wakajenga kama amri ilivyotolewa na Mungu wa Israel na Koreshi, Dario
na Artashasta mfalme wa Uajemi. 15 Nyumba ikakamilika siku ya tatu ya mwezi
wa adari, katika mwaka wa sita wa kutawala mfalme Dario. 16 watu wa Israel,
makuhani, walawi na watu waliobaki wa uhamisho wakasheherekea kuweka wakfu
nyumba ya Mungu kwa furaha. 17 Wakatoa ngombe mia moja, kondoo mia moja
na kondoo wengine mia nne kwa ajili ya kuweka wakfu nyumba ya Mungu. Mbuzi
wa kiume kumi na wawili walitolewa kama sadaka ya dhambi kwa ajili ya waisrael
wote kila kabila katika Israel. 18 Pia wakawapa wajibu makuhani na walawi kufanya
mgawanyo wa kazi ya Mungu katika Yerusalem. Kama ilivyoandikwa katika kitabu
cha Musa. 19 Hivyo wale waliokuwa utumwani wakasherehekea pasaka siku ya kumi
na nne ya mwezi wa kwanza. 20 Makuhani na walawi wakajitakasa wenyewe na
wakachinja pasaka ya sadaka kwa ajili ya waliokuwa mateka wakiwemo na wao
wenyewe. 21 watu wa Israel ambao walikula nyama ya Pasaka ni wale waliorudi
kutoka uhamishoni na walikuwa wamejitenga wenyewe kutoka kwa watu wasio safi
wa nchi ile na kumchagua Yahwe, Mungu wa Israel. 22 Walifurahi na kushangilia
siku kuu ya mikate isiyochacha kwa siku saba, kwa sababu Yahwe amewarejeshea
furaha na ameugeuza moyo wa mfalme wa Ashuru, na kuwatia nguvu kwa kazi ya
nyumba, nyumba ya Mungu wa Israel.

# 7

1 Sasa baada ya hili, kipindi cha kutawala Artashasta mfalme wa Uajemi, Ezra akaja
kutoka Babeli. Watangulizi wa Ezra walikuwa: Seraya, Azaria, Hilkia, 2 Shalumu,
Sadoki, Ahitubu, 3 Amaria, Azaria, Merayothi, 4 Zerahia, Uzi, Buki, 5 Abishaua, Fineasi,
Eliazari ambaye ni mtoto wa Haruni kuhani mkuu. 6 Ezra akaja kutoka Babeli na
alikuwa mtalaam mwandishi wa sheria ya Musa, ambayo Yahwe, Mungu wa Israel
aliwapa. Mfalme akampatia kila kitu alichooomba kwa kuwa mkono wa Yahwe
ulikuwa pamoja naye. 7 Baadhi ya wazao wa Israel, na makuhani, walawi, waimbaji,
walinzi, na wale waliochaguliwa kuhudumu katika Hekalu pia wakaenda Yerusalem
katika mwaka wa saba wa mfalme Artashasta. 8 Naye akafika Yerusalem mwezi
wa tano kama mwaka huo. 9 Naye akaondoka Babeli siku ya kwanza ya mwezi wa

kwanza. Ilikuwa siku ya kwanza ya mwezi wa tano ambapo alifika Yerusalem, kwa
kuwa mkono mzuri wa Mungu ulikuwa pamoja naye. [10] Ezra alikuwa ametoa moyo
wake kusoma, kutenda, na kufundisha maagizo na sheria za Yahwe. [11] Hii ndio amri
ambayo mfalme Artashasta alimpa Ezra kuhani na mwandishi wa sheria za Yahwe na
maagizo kwa Israeli. [12] Mfalme wa wafalme Artashasta, kwa kuhani Ezra, mwandishi
wa sheria za Mungu wa mbinguni. [13] Ninatoa amri kwamba mtu yeyote Israel
katika ufalme wangu pamoja na makuhani na walawi ambao wanatamani kwenda
Yerusalem, wanaweza kwenda pamoja na wewe. [14] Mimi mfalme na washauri wangu
saba, tunawatuma wote kwenda kufahamu kuhusu Yuda na Yerusalem kuhusiana na
sheria ya Mungu, ambayo iko mkononi mwako. [15] Itakupasa kuleta Dhahabu na fedha
ambazo walitoa kwa ajili ya Mungu wa Israel, ambaye makazi yake ni Yerusalem.
[16] Fedha iliyotolewa kwa hiari na Dhahabu yote iliyotolewa Babeli pamoja na matoleo
ya hiari waliotoa watu na makuhani kwa ajili ya nyumba ya Mungu katika Yerusalem.
[17] Basi ununue vyote sadaka ya kondoo, beberu, kondoo, unga na kinywaji, uvitoe
kwenye madhabahu ambayo ni nyumba ya Mungu wako katika Yerusalem. [18] Fanya
hivyo pamoja na sehemu ya fedha na dhahabu, vyovyote utakavyoona inakupendeza
wewe na ndugu zako, kumpendeza Mungu. [19] Viweke vitu vilivyotolewa kwa hiari
mbele yako kwa ajili ya huduma ya nyumba ya Mungu Yerusalem. [20] Kitu chochote
kingine ambacho kinahitajika kwenye nyumba ya Mungu wako ambacho unahitaji,
Gharama yake itatoka kwenye hazina yangu. [21] Mimi mfalme Artashasta, natoa
amri kwa wotunza hazina wote mjini ngambo ya mto, chochote Ezra atakachoomba
kwenu anapaswa kupewa chote, [22] hata zaidi ya talanta mia moja za fedha, vipimo
mia vya ngano, bathi mia za divai na bathi mia za mafuta, pia na chumvi isiyo
na kikomo. [23] Chochote ambacho kimeamriwa kutoka kwa Mungu wa mbinguni,
kifanye hicho kwa utukufu wa nyumba yake. Kwa nini hasira yake ije kwenye
ufalme wangu na watoto wangu? [24] Tutawapa taarifa wao kuhusu ninyi kwamba
wasiwatoze ushuru wowote au kodi kwa kuhani, mlawi, mwimbaji, mlinzi au kwa
mtu aliyechaguliwa kwenye huduma ya Hekalu na mtumishi katika nyumba ya
Mungu. [25] Ezra, kwa hekima aliyokupa Mungu, inakulazimu kuteua waamuzi na mtu
muelewa kuwahudumia watu katika mji ngambo ya mto na kusaidia yeyote anayejua
sheria za Mungu wako. Pia inakubidi ufundishe wale ambao hawajui sheria. [26] Toa
adhabu kwa yeyote asiyetii sheria ya Mungu au sheria ya mfalme, ikiwezekana kwa
kifo, kuhamishwa, kuchukuliwa mali zake au kufungwa. [27] Atukuzwe, Yahwe, Mungu
wa watangulizi wetu, ambaye aliweka ndani ya moyo wa mfalme ili kutuza Nyumba
ya Yahwe Yerusalem, [28] ambaye akaendeleza agano kwangu kwa uaminifu mbele
ya mfalme, na washauri wake na wakuu wake wenye mamlaka, nilitiwa nguvu
na mikono ya Yahwe, Mungu wangu, nami nikawakusanya viongozi kutoka Israel
kwenda pamoja nami.

# 8

[1] Hawa ni viongozi wa watangulizi familia ambazo zilitoka babeli pamoja nami
kipindi cha utawala wa mfalme Artashasta. [2] Mwana wa Finehasi, Gershoni. Mwana
wa Ithamari, Daniel. Mwana wa Daudi, Hatushi ambaye ni mwana Shekania,
[3] ambaye pia ni mwana wa Paroshi na Zekaria na pamoja na yeye kulikuwa na
wanaume mia moja na hamsini walitajwa kwenye idadi ya ukoo wake. [4] Wana wa
Pahath- Moabu, Eliehoenai mwana wa Zerahia na pamoja naye wanaume mia mbili.
Wana wa [5] Shekaniah, Yahazieli na pamoja naye wanaume mia tatu. Wana wa [6] adini,
Ebedi mwana wa Yonathani na pamoja naye waliorodheshwa wanaume hamsini.
[7] Wana wa Elamu, Yeshaya mwana wa Athalia na pamoja naye waliorodheshwa
wanaume sabini. [8] Wana wa Shefatia, Zebadia, mwana wa Mikaeli na pamoja naye

waliorodheshwa wanaume themanini. 9 Wana wa Yoabu, Obadia mwana wa Yehieli
pamoja na yeye waliorodheshwa wanaume mia mbili kumi na wanane. Wana wa
Binui, 10 Sheromithi, mwana wa Yosifia na pamoja na yeye waliorodheshwa wanaume
mia moja na sitini. 11 Wana wa Bebai, zekaria mwana wa Bebai na pamoja na
yeye waliorodheshwa wanaume ishirini na wanane. 12 Wana wa Azgadi, Yohana
mwana wa Hakatani na pamoja na yeye waliorodheshwa wanaume mia moja na
kumi. 13 Wale wana wa Adonikamu wakaja baadaye. Na haya ndio majina yao:
Elifereti, Yeueli na Shemaya na pamoja na wao wakaja wanaume sitini. 14 Wana
wa Bigwai, Uthai, mwana wa zabudi na pamoja na yeye waliorodheshwa wanaume
sabini 15 Nikawakusanya wasafiri bandari iliyokuwa inaelekea Ahava. Tukaweka
kambi muda wa siku tatu, nikawachunguza watu na makuhani, lakini sikuwaona
wana wa Levi miongoni. 16 Hivyo nikatuma kwa Eliezeri, arieli, Shemaya, Elnathani,
Yaribu na Elnathani na Nathani, Zekaria na Meshulamu waliokuwa viongozi na
kwa Yoyaribu na Elnathani ambao walikuwa ni walimu. 17 Tena nikawatuma kwa
Ido, kiongozi wa Kasifia. Nikawaaambia kile watachomweleza Ido. na jamaa zake,
watumishi wa Hekalu waliishi Kasifia, kwa hiyo, kutuma kwetu watumishi kwa ajili
ya nyumba ya Mungu. 18 Hivyo wakatutuma sisi kwa Mungu na mkono mzuri wa
mtu aliyeitwa Ishekeli. Alikuwa mwana wa mali Mwana wa Levi mwana wa Israel.
Akaja na wana kumi na wanane na ndugu, 19 pamoja naye Hashabia, pamoja na
Yeshaya wa wana wa Merari na ndugu zake na wana wake jumla watu ishirini wote.
Miongoni 20 mwao walichaguliwa kutumika katika Hekalu, ambapo Daudi na wakuu
waliwapa kuwahudumia walawi: mia mbili ishirini kila mmoja wao aliagizwa kwa
majina. 21 Tena nikatangaza kufunga mto Ahava ili kujinyenyekeza mbele za Mungu,
kutafuta njia iliyoonyoka kutoka kwake kwa ajili yetu, watoto wetu na mali zetu,
22 Niliona aibu kumwomba mfalme kwa ajili ya jeshi au mpandafarasi kwa ajili ya
kutulinda tunapokuwa njiani, tangu tumemwambia mfalme "mkono wa Mungu uko
pamoja na wote wanaomtafuta kwa mazuri. lakini uweza wake na ghazabu yake
ni juu ya wale wote wanaomwasi yeye. 23 Hivyo tulifunga na kumsihi Mungu kwa
jambo hilo. 24 Tena nikachagua watu kumi na wawili kutoka kwa kuhani: Sherebia na
Hashabia na ndugu zao wengine kumi. 25 Nikapima kwa ajili yao fedha, dhahabu na
vyombo na sadaka kwa ajili ya nyumba ya Mungu kwa wafalme, washauri, na wakuu
na Israel wote walitoa kwa hiari. 26 Hivyo nikawapimia kwenye mikono yao talanta
za fedha mia sita na hamsini, talanta mia moja ya vyombo vya fedha, talanta mia
moja za dhahabu. 27 vifaa ishirini vya dhahabu kwa pamoja vilikuwa na thamani
ya elfu moja darkoni na vitu viwili vya sanamu vivyonakshiwa kama dhahabu ya
kupendeza. 28 Kisha nikawaambia, mmewekwa wakfu kwa Bwana, na hivi vyombo
pia na fedha na dhahabu, vimetolewa kwa hiari kwa Yahwe, Mungu wa watangulizi
wenu. 29 mviangalie na kuvitunza hadi mtakapovipima mbele ya makuhani, walawi,
na viongozi wa wataangulizi wa jamii ya Israel katika Yerusalem katika nyumba ya
Mungu. 30 Makuhani na walawi walikubali vipimo vya fedha na dhahabu na vyombo
kwa ajili ya kuvichukua na kuvipeleka Yerusalem, kwenye nyumba ya Mungu wetu.
31 Tukatoka kwenda mto Ahava siku ya kumi na mbili katika mwezi wa kwanza
kwenda Yerusalem, Mkono wa Mungu ulikuwa pamoja nasi, ulitulinda na mikono
ya adui na wale waliotaka kutufanyia fujo njiani. 32 Hivyo tukaingia Yerusalem
na kukaa humo kwa siku tatu. 33 Tena siku ya nne fedha na dhahabu na vyombo
vilipimwa ndani ya nyumba ya Mungu wetu kwa mikono ya Meremothi mwana
wa Uria kuhani, na pamoja nao alikuwepo Eleazari mwana wa Finehasi, Yozabadi
mwana wa Yeshua, na Noadia mwana wa Binui, Walawi. 34 Idadi na uzito wa kila
kitu uliweza kujulikana. Uzito wote uliweza kuandikwa katika kipindi hicho 35 Na
wale waliokuja kutoka matekani, watu wa uhamisho, wakatoa sadaka ya kutekezwa

kwa Mungu wa Israel, kondoo tisini na sita, wana-kondoo sabini na saba na mbuzi wa
kiume kumi na wawili kama sadaka ya dhambi. Zote zilikuwa sadaka za kutekezwa
kwa ajili ya Yahwe. 36 Tena wakawapa amri za mfalme kwa wakuu wa wafalme na
wakuu katika mji ngambo ya mto, na wakawasaidia watu na nyumba ya Mungu.

# 9

1 Kipindi mambo hayo yanatendeka, wakuu wakaja kwangu na kuniambia,"Watu
wa Israel, Makuhani na walawi hawakuweza kujitenga wenyewe kutoka kwa watu
wa nchi zingine na maovu yao: Wakanaani, Wahiti, Waperuzi, wayebusi, Waamoni,
Wamoabu, Wamisri na Waamori. 2 Kwa kuwa wamewachukua baadhi ya binti na
watoto wa kiume, wamejichanganya watu watakatifu na watu wa nchi nyingine na
wakuu na viongozi wamekuwa wa kwanza katika imani hii potofu. 3 Niliposikia
haya, nikachana nguo zangu na kanzu na kunyoa nywele kichwani na ndevu na
nikakaa chini kutafakari. 4 Na wale wote waliotetemeka kwa neno la Mungu wa Israel
kuhusu imani potofu walikusanyika kwangu wakati nimakaa chini nikiwa na aibu
hadi kufikia kipindi cha sadaka za jioni. 5 Lakini katika sadaka ya jioni nikasimama
kwenye nafasi yangu nikiwa mnyenyekevu na nguo ilichanika na kanzu, na nikapiga
magoti na kunyoosha mikono yangu kwa Yahwe Mungu wangu. Nikasema 6 "Mungu
wangu, nina aibu na sistahili kuinua uso wangu kwako, makosa yetu yamekuwa
hadi kuvuka kichwani na maovu yetu yameongezeka kufika mbinguni. 7 Kuanzia
siku ya watangulizi wetu mpaka sasa tumekuwa katika maovu makuu. Makosa
yetu, viongozi, makuhani, walikuwa katika mikono ya mfalme wa dunia hii, katika
upanga, matekani na kunyanyaswa na tuna aibu ya uso hata leo. 8 sasa kwa kipindi
kifupi, neema kutoka kwa Yahwe Mungu wetu imekuja kutuacha mabaki wachache
na kutupa kuhimmili sehemu takatifu. Hii ilikuwa ni kwa ajili ya Mungu wetu
kututia nuru macho yetu na kutupa unafuuu sisi tulio watumwa. 9 Kwa kuwa sisi
tu watumwa, lakini Mungu bado hajatusahau lakini ameongeza agano la uaminifu
kwetu, ameyatenda haya mbele ya macho ya mfalme wa Uajemi ili kwamba haweze
kutupatia nguvu mpya. Ili kwamba tuweze kujenga nyumba ya Mungu na tuweze
kuondoa majuto. Alitenda hayo ili kwamba aweze kutupatia msingi wa usalama
katika Yuda na Yerusalem. 10 Lakini sasa Mungu wetu, tuseme nini baaada ya haya?
Tumesahau amri zako. 11 amri ambazo uliwapa manabii watumishi wako, pale
uliposema, "Nchi hii mnayoingia kuimiliki ni nchi chafu. Imechanganyikana na watu
wasio na utaratibu. ameenea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa uchafu wao.
12 Hivyo sasa, msiwape binti zenu kwa watoto wao, msichukue binti zao kwa ajili ya
watoto wenu, msitafute amani kwao na fadhili, ili kwamba muweze kuwa imara na
kula vizuri vya nchi, hivyo utasababisha watoto wenu kumiliki kwa wakati wote."
13 Baada ya yote kutokea kwetu kwa sababu ya uovu wetu na makosa yetu makuu,
tokea hapo, Mungu wetu, hukutazama makosa yetu na kutuadhibu tulivyostahili
na ukatuacha kama mabaki. 14 Tunaweza kuvunja tena amri zako na kuingiliana
katika ndoa, na hawa watu wasiofuata utaratibu? Je hautachukia na kututowesha
sote hakuna wa kubaki, hakuna wa kutoroka? 15 Yahwe, Mungu wa Israel, wewe ni
mwenye haki, kwa kuwa tumebaki wachache mabaki hadi siku ya leo. Tazama, tuko
mbele yako na makosa yetu, kwa kuwa hakuna hata mmoja anayeweza kusimama
mbele kwa sababu ya hili.

# 10

1 Wakati Ezra akiomba na kutubu, akalia na kujirusha chini mbele ya nyumba ya
Mungu, kusanyiko kubwa la wanaume Israel, wanawake na watoto wakakusanyika
kwake, kwa kuwa watu walikuwa wakilia sana. 2 Shekania mtoto wa Yehieli, mwana

wa Elamu akamwambia Ezra, “Tumekuwa sio waaminifu kwa Mungu na tumeoa
wanawake wa kigeni kutoka nchi nyingine. Lakini pamoja na hilo, bado kuna
tumaini kwa Israel. 3 sasa natuweke agano pamoja na Mungu wetu kuwaondoa
wanawake wote na watoto wao kulingana na maelekezo ya Bwana, na maelekezo
ya wale wanaotetemeka kutokana na amri za Mungu wetu. na hii ifanyike kutokana
na sheria. 4 Simama, jambo hili linakuhusu wewe, na sisis tuko pamoja na wewe,
Uwe imara na kufanya hili. 5 Hivyo Ezra akasimama na kufanya makuhani na
walawi na waisrael wote wakaahidi kufanya kwa njia hiyo. Hivyo wote wakatoa
kiapo. 6 Ndipo Ezra akainuka kutoka mbele ya nyumba ya Mungu na kwenda kwenye
chumba ya Yehohanani mtoto wa Eliashibu, Yeye hakula mkate au kunywa maji.
Tangu alipokuwa akiomboleza kuhusiana na wale wenye imani haba waliokuwa
uhamishoni. 7 Hivyo wakatuma neno katika Yuda na Yerusalem kwa watu wote
waliorudi kutoka utumwani kukusanyika Yerusalem. 8 Yeyote ambaye hakuja katika
siku tatu kutokana na maelekezo kutoka kwa wakuu na viongozi atachukuliwa mali
zote na atatengwa na kusanyiko kuu la watu ambao walikuja kutoka uhamisho.
9 Hivyo watu wote wa Yuda na Benjamini wakakusanyika Yerusalem kwa siku tatu.
Ilikuwa ni mwezi wa tisa na siku ya ishirini ya mwezi. watu wote wakasimama
mbele ya nyumba ya Mungu na wakatetemeka kwa sababu ya neno na mvua. 10 Ezra
kuhani akasimama na kusema, “Ninyi wenyewe mmefanya uasi, ninyi mmeishi na
wanawake wa kigeni na kuongeza makosa ya Israel. 11 Lakini sasa mpeni sifa
Yahwe, Mungu wa watangulizi wenu, na mfanye mapenzi yake, mjitenge na watu
wa nchi na wanawake wa kigeni. 12 Kusanyiko lote likajibu kwa sauti. “Tutatenda
kama ulivyosema, 13 haijalishi, kuna watu wengi na ni kipindi cha mvua. Hatuna
nguvu ya kusimama nje na hii si siku moja au mbili za kufanya kazi, kwa kuwa
tumekosea katika jambo hili. 14 Hivyo wakuu wetu wawakilishe kusanyiko lote,
iwe kwamba wote walioruhusu wanawake wa kigeni kuishi katika miji yetu waje
katika muda uliopangwa na viongozi wa mji na waamuzi wa mji hadi hapo hasira ya
Mungu itakapoondoka kutoka kwetu. 15 Yonathan mtoto Asaheli na Yazeya mwana
wa Tikwa wakapinga hili, Meshulamu na Shabethai mlawi wakawaunga mkono
wao. 16 Hivyo watu waliotoka uhamishoni wakafanya hivi, Ezra kuhani akachagua
wanaume, viongozi watamgulizi wa ukoo na nyumba, wao wote kwa majina na
wakaliangalia suala hili siku ya kwanza ya mwezi wa kumi. 17 Siku ya kwanza ya
mwezi wa kwanza wakawa wamemaliza kuchunguza wale wanaume walioishi na
wanawake wa kigeni. 18 Miongoni mwa wana wa kikuhani kuna wale walioishi na
wanawake wa kigeni. Miongoni mwa wana wa Yoshua mtoto wa Yosadaki na kaka
zake ambao walikuwa Maasela, Eliazeri, na Yaribu na Gedalia. 19 Hivyo wakaamua
kuwaondoa wake zao. kwa kuwa walikuwa na makosa, wakatoa sadaka ya kondoo
kwenye mifugo kwa ajili ya makosa yao. 20 Miongoni mwa wana wa Imeri, Hanani,
na Zebadia. 21 Miongoni mwa wana wa Harimu, Maaseya, na Eliya na Shemaya,
na Yehieli na Uzia. 22 Miongoni mwa wana wa Pashuri, Elasa 23 Miongoni mwa
walawi: Yozabadi na Shimei na Kelaya (ndiye Kelita) na Pethaia, na Yuda na Eliezeri.
Miongoni mwa waimbaji Eliashibu na. Miongoni mwa walinzi Shalumu, Telemu na
Uri. 24 Miongoni mwa Israel waliobaki - 25 Miongoni mwa wana wa Paroshi, Ramia na
Izia na Malkiya na Miyamini na Eliazari na Malkiya na Benaya 26 Miongoni mwa wana
wa Elamu Mataniana Zekaria, na yeehieli, na Abdi na Yeremothi na Eliya. 27 Miongoni
mwa wana wa Zatu: Elionai, na Eliashibu, na Matania na Yeremothi na Zabadi na
Aziza. 28 Miongoni mwa wana wa Bebai Yehohanani, na Hanania na Zakai na Athlai.
29 Miongoni mwa wana wa bani: Meshulami na Maluki, na Adaya na Yashubu na
Sheali na Yeremothi. 30 Miongoni mwa wana wa Pahath-Moabu, Adna, na kelali, na
Benaya na Maaseya, na Matania, na Besaleli na Binti na Manase. 31 Na miongoni

mwa wana wa Harimu: Eliezeri na Ishiya, na Malkiya na Shemaya na Shimeoni, na
32 Benyamini na Maluki na Shemaria 33 Miongoni mwa wana Hashumu: Matenai, na
Matatana Zabadi, na Elifereti na Yeremai, na Manase, na Shimei. 34 Miongoni mwa
wana wa Bani: Maadai, na Amramu na Aueli, na 35 Benaya, na Bedeya na Keluhi,
na 36 wania, na Meremothi, Eliashibu, 37 Matania, na Matenai. na 38 Yaasi. Miongoni
mwa wana wa Binui: Shimei, 39 Sheremia, na Nathani, na Adaya, na 40 Maknadebai,
na Shashai, na Sharai 41 Azareri, na Sheremia, na Shemaria, na 42 Shalumu, na
Amaria, na Yusufu. 43 Miongoni wa wana wa Nebo: Yeieli, na Mathiana zabadi, na
Zebina, na Ido, na Yoeli na Benaya. 44 Hawa wote walikuwa wameoa wanawake wa
kigeni na walikuwa wamezaa watoto baadhi yao.

# Nehemia

1 Maneno ya Nehemia mwana wa Hakalia Ikawa, katika mwezi wa Kisleu, katika
mwaka wa ishirini, nilikuwa katika mji mkuu wa Sushani, 2 mmoja wa ndugu zangu,
Hanani, alikuja pamoja na watu wengine kutoka Yuda, nami nikawauliza kuhusu
Wayahudi waliopona, Wayahudi waliosalia waliokuwa huko, na kuhusu Yerusalemu.
3 Wakaniambia, “Wale waliokuwa katika mkoa ule waliookoka katika kifungo wapo
katika shida kubwa na aibu kwa sababu ukuta wa Yerusalemu umebomolewa na
milango yake imeteketezwa kwa moto.” 4 Na mara tu niliposikia maneno haya,
nikakaa na kulia, na kwa siku niliendelea kuomboleza na kufunga na kuomba
mbele ya Mungu wa mbinguni. 5 Ndipo nikasema, “Wewe ndiwe Bwana, Mungu
wa mbinguni, Mungu uliye mkuu na kushangaza, unayetimiza agano na upendo wa
kudumu pamoja na wale wanaokupenda na kushika amri zake. 6 Sikiliza maombi
yangu na fungua macho yako, ili uisikie sala ya mtumishi wako kwamba sasa nasali
mbele yako mchana na usiku kwa ajili ya watu wa Israeli watumishi wako. Mimi
ninakiri dhambi za watu wa Israeli, ambazo tumefanya dhidi yako. Wote mimi na
nyumba ya baba yangu tumefanya dhambi. 7 Tumefanya uovu sana juu yako, na
hatukuzingatia amri, sheria, na hukumu ambazo ulimwamuru mtumishi wako Musa.
8 Tafadhali kumbuka neno ulilomuamuru mtumishi wako Musa, 'mkitenda pasipo
uaminifu, nitawatawanya kati ya mataifa, 9 lakini mkirudi kwangu na kufuata amri
zangu na kuzifanya, ingawa watu wako walienea chini ya mbingu za mbali, Nami
nitawakusanya kutoka huko na kuwaleta mahali pale nilipopachagua ili kulifanya
jina langu.' 10 Sasa wao ni watumishi wako na watu wako, ambao uliwaokoa kwa
nguvu yako kubwa na kwa mkono wako wenye nguvu. 11 Bwana, naomba, sikiliza
sasa maombi ya watumishi wako na sala ya watumishi wako ambao hufurahia
kuheshimu jina lako. Sasa unifanikishe mimi mtumishi wako leo, na unijalie rehema
mbele ya mtu huyu.” Nilikuwa mnyweshaji wa mfalme.

## 2

1 Katika mwezi wa Nisani, katika mwaka wa ishirini wa mfalme Artashasta,
alichagua divai, na nikachukua divai na kumpa mfalme. Sasa sikuwahi kusikitikaa
mbele yake. 2 Lakini mfalme akaniambia, “Kwa nini uso wako una huzuni?
Hauonekani kuwa mgonjwa. Hii lazima iwe huzuni ya moyo.” Kisha nikaogopa
sana. 3 Nikamwambia mfalme, “Mfalme aishi milele! Kwa nini uso wangu usiwe
na huzuni? ikiwa mji, mahali pa makaburi ya baba yangu, uko katika magofu, na
malango yake yameharibiwa kwa moto.” 4 Ndipo mfalme akaniambia, “Unataka nini
nifanye?” Kwa hiyo nikamwomba Mungu wa mbinguni. 5 Nikamwambia mfalme,
“Mfalme akiona vema, na ikiwa mtumishi wako amefanya vizuri machoni pako,
unaweza kunituma Yuda, mji wa kaburi za baba zangu, ili nipate kuujenga tena.”
6 Mfalme akanijibu (na malkia pia alikuwa amekaa karibu naye), “Utakaa kawa
muda gani mpaka urudi?” Mfalme akaona vema kunipeleka nami nikampka muda.
7 Ndipo nikamwambia mfalme, “Ikiwa itampendeza mfalme, nipe barua kwa ajili
ya wakuu ng'ambo ya Mto, ili wapate kuniruhusu nipite katika maeneo yao njiani
kwenda Yuda. 8 Pia iwepo barua kwa Asafu, mlinzi wa msitu wa mfalme, ili anipe
miti ya kufanya mihimili ya malango ya ngome karibu na hekalu, na kwa ukuta
wa mji, na kwa nyumba ambayo Nitaishi.” Kwa hiyo kwa sababu mkono mzuri
wa Mungu ulikuwa juu yangu, mfalme alinipa hitaji langu. 9 Nilifika kwa wakuu
ng'ambo ya Mto, na kuwapa barua za mfalme. Basi mfalme alikuwa amepeleka

maofisa wa jeshi na wapanda farasi pamoja nami. 10 Sanbalati Mhoroni na Tobbia
mtumishi wa Amoni waliposikia jambo hili, walipendezwa sana kwa kuwa mtu
alikuja ambaye alikuwa akijaribu kuwasaidia watu wa Israeli. 11 Basi, nikarudi
Yerusalemu, na nilikuwa huko siku tatu. 12 Niliamka usiku, mimi na watu wachache
pamoja nami. Sikumwambia mtu yeyote kile Mungu wangu alichoweka ndani ya
moyo wangu kufanya Yerusalemu. Hakukuwa na mnyama pamoja nami, isipokuwa
yule niliyekuwa nimempanda. 13 Niliondoka usiku kwa njia ya lango la bondeni,
kuelekea kisima cha joka na kwenye mlango wa jaa, na kukagua kuta za Yerusalemu,
ambazo zimebomolewa, na milango ya mbao iliharibiwa na moto. 14 Kisha nikaenda
kwenye lango na Chemchemi ya Mfalme. Nafasi ilikuwa nyembamba sana kwa
mnyama niliyekuwa nimempanda kupita. 15 Kwa hiyo nilikwenda usiku huo kando
ya bonde na kuchunguza ukuta, nikarudi nyuma na kuingia kwa lango la bondeni,
na hivyo nikarudi. 16 Watawala hawakujua nilipokwenda au kile nilichofanya, na
sikuwaambia Wayahudi, wala makuhani, wala wakuu, wala watawala, wala wengine
waliofanya kazi hiyo. 17 Nikawaambia, "Unaona shida tuliyo nayo, jinsi Yerusalemu
iko katika magofu na milango yake imeharibiwa kwa moto. Njoni, tujenge upya
ukuta wa Yerusalemu, ili tusiwe na aibu tena." 18 Niliwaambia kuwa mkono mzuri
wa Mungu wangu ulikuwa juu yangu na pia kuhusu maneno ya mfalme ambayo
aliniambia. Wakasema, "Hebu tuondoke na kujenga." Kwa hiyo wakaimarisha
mikono yao kwa ajili ya kazi nzuri. 19 Lakini Sanbalati Mhoroni, na Tobia mtumishi
wake Mwamoni, na Geshemu, Mwarabu, waliposikia habari hiyo, wakatucheka na
kututukana; wakasema, "Unafanya nini? Je, unamgombana na mfalme?" 20 Ndipo
nikawajibu, "Mungu wa mbinguni atatupa ufanisi. Sisi ni watumishi wake na
tutaondoka na kujenga. Lakini huna sehemu, hakuna haki, na hakuna dai la
kihistoria huko Yerusalemu."

# 3

1 Kisha Eliashibu, kuhani mkuu, akasimama pamoja na ndugu zake makuhani,
wakajenga lango la kondoo. Walitakasa na kuweka milango yake. Waliweka wakfu
hadi mnara wa Hamea na hadi mnara wa Hananeli. 2 Baada yao watu wa Yeriko
walijenga, na baada yao Zakuri mwana wa Imri alijenga. 3 Wana wa Senaa wakajenga
lango la samaki. Wanaweka mihimili yake na kuweka milango yake na vyuma vyake
na makomeo yake. 4 Meremoth aliandaa sehemu inayofuata. Yeye ni mwana wa
Uria mwana wa Hakosi. Na baada yao Meshulamu akatengeneza. Yeye ni mwana wa
Berekia mwana wa Meshezabeli. Karibu nao Sadoki akatengeneza. Yeye ni mwana
wa Baana. 5 Baada yao Watekoi wakatengeneza, lakini viongozi wao walikataa
kufanya kazi iliyoagizwa na wakuu wao. 6 Yoyada mwana wa Pasea, na Meshulamu
mwana wa Besodeya, walitengeneza lango la Kale. Wanaweka mihimili, na kuweka
milango yake na vyuma vyake na makomeo yake. 7 Nao, Melatia Mgibeoni, na Yadoni
Meronothi, watu wa Gibeoni na Mispa, walifanyia matengenezo juu ya sehemu
ambapo mkuu wa mkoa wa ng'ambo ya Mto aliishi. 8 Na baada yake Uzieli mwana
wa Harhaya, mmoja wa wafua dhahabu, akatengeneza; na baada yake Hanania,
mtengenezaji wa manukato. Wakajenga tena Yerusalemu mpaka Ukuta mpana. 9 Na
baada yao Refaya mwana wa Huri akajenga. Alikuwa mtawala wa nusu ya wilaya
ya Yerusalemu. 10 Na baada yao Yedaya mwana wa Harumafu akajenga karibu na
nyumba yake. Na baada yake Hatushi mwana wa Hashabneya akajenga. 11 Malkiya
mwana wa Harimu na Hashubu mwana wa Pahat Moabu, wajenga sehemu nyingine
pamoja na mnara wa tanuu. 12 Baada yao Shalumu mwana wa Haloheshi, mkuu wa
nusu ya wilaya ya Yerusalemu, akajenga, pamoja na binti zake. 13 Hanuni na wenyeji
wa Zanoa walijenga lango la bondeni. Walijenga tena na kuweka milango yake, na

vyuma vyake na makomeo yake. Walijenga dhiraa elfu hadi lango la jaa. [14] Malkiya,
mwana wa Rekabu, mkuu wa wilaya ya Beth-Hakeremu, akajenga lango la jaa.
Alijenga na kuweka milango yake, na vyuma vyake na makomeo yake. [15] Shalumu
mwana wa Kolhoze, mkuu wa wilaya ya Mispa, akajenga lango la Chemchemi.
Alijenga, na kuweka kifuniko juu yake na kuweka milango yake na vyuma vyake
na makomeo yake. Alijenga upya ukuta wa Pwani wa Silowamu kwa bustani ya
mfalme, hadi ngazi ya kuongoza kutoka mji wa Daudi. [16] Nehemia mwana wa Azbuki,
mtawala wa nusu ya wilaya ya Beth-suri, akajenga mahali hapo, toka maburini ya
Daudi, mpaka birika lililojengwa na watu, na nyumba ya watu wenye nguvu. [17] Baada
yake, Walawi walijenga, pamoja na Rehumi mwana wa Bani na baada yake, Hashabia,
mtawala wa nusu ya wilaya ya Keila, kwa wilaya yake. [18] Baada yake watu wa
nchi zao walijenga, ikiwa ni pamoja na Binui mwana wa Henadadi, mkuu wa nusu
ya wilaya ya Keila. [19] Baada yake alijenga Ezeri, mwana wa Yeshua, mtawala wa
Mispa, alijenga sehemu nyingine kuelekea ghala ya silaha, kwenye kona ya ukuta.
[20] Baada yake Baruki, mwana wa Zakai, akajenga kwa hiari sehemu nyingine, toka
kona ya ukuta mpaka mlango wa nyumba ya Eliashibu, kuhani mkuu. [21] Baada yake
Meremothi, mwana wa Uria, mwana wa Hakosi, akajenga sehemu nyingine, toka
mlango wa nyumba ya Eliashibu mpaka mwisho wa nyumba ya Eliashibu. [22] Kisha
baada yake makuhani, watu wa eneo hilo karibu na Yerusalemu, walijenga. [23] Baada
yao Benyamini na Hashubu walijenga kuielekea nyumba yao. Baada yao Azaria
mwana wa Maaseya, mwana wa Anania, alijenga karibu na nyumba yake. [24] Baada
yake Binui mwana wa Henadadi akajenga sehemu nyingine, kutoka nyumba ya
Azaria hadi kona ya ukuta. [25] Palali, mwana wa Uzai, akajenga juu ya kona ya ukuta
na mnara unaoenea juu kutoka nyumba ya juu ya mfalme katika uwanda wa walinzi.
Baada yake Pedaya mwana wa Paroshi akajenga. [26] Sasa watumishi wa hekalu
waliokaa Ofeli walijenga mpaka upande wa Hifadhi ya Maji upande wa mashariki
wa mnara unaojitokeza. [27] Baada yake, Watekoi walijenga sehemu nyingine, kuelekea
mnara mkubwa ulio nje, mpaka ukuta wa Ofeli. [28] Makuhani wakajenga juu ya lango
la farasi, kila mmoja kuelekea nyumba yake. [29] Baada yao Sadoki, mwana wa Imeri,
alijenga sehemu hiyo kuelekea nyumba yake. Na baada yake Shemaya mwana wa
Shekania, mlinzi wa lango la mashariki, akajenga. [30] Baada yake Hanania, mwana
wa Shelemia, na Hanuni, mwana wa sita wa Salafu, wakajenga sehemu nyingine.
Meshulamu mwana wa Berekia akajenga kuelekea kwenye vyumba vyake. [31] Baada
yake Malkiya, mmoja wa wafua dhahabu, akajenga mpaka nyumba ya watumishi
wa hekalu na wafanyabiashara waliokuwa wakielekea lango la gereza na mpaka
chumba cha juu cha pembeni. [32] Wafanyabiashara wa dhahabu na wafanyabiashara
walijenga kati ya chumba cha juu cha kona na Lango la Kondoo.

# 4

[1] Sanbalati alipoposikia tulikuwa tukijenga ukuta, akaghadhabika ndani yake, naye
akakasirika sana, akawacheka Wayahudi. [2] Mbele ya ndugu zake na jeshi la Samaria,
akasema, “Wayahudi dhaifu hawa wanafanya nini? Je, watajifanyia mji wenyewe?
Je, watatoa dhabihu? Je, wataimaliza kazi siku moja? Je! Watawaletea mawe
kutoka kwenye kifusi baada ya kuchomwa moto? [3] Tobia Mwamoni alikuwa pamoja
naye, naye akasema, 'Ikiwa tu mbweha angepanda juu ya hichi wanachokijenga,
angeubomoa ukuta huo wa mawe.” [4] Tusikilize, Mungu wetu, kwa maana sisi
tunatukanwa. Rudisha malalamiko yao juu ya vichwa vyao wenyewe na kuwapa
wapate kutekwa katika nchi ambapo wao ni wafungwa. [5] Usiufunike uovu wao,
wala usiondoe dhambi zao mbele yako; kwa sababu wamewachukiza wanaojenga.
[6] Kwa hiyo tulijenga ukuta na ukuta wote uliunganishwa kwa nusu ya urefu wake,

kwa kuwa watu walikuwa na hamu ya kufanya kazi 7 Lakini Sanbalati, Tobia,
Waarabu, Waamoni, na Waashdodi waliposikia kwamba kazi ya ukarabati wa kuta
za Yerusalemu ilikuwa ikiendelea, na kwamba sehemu zilizovunjika katika ukuta
zilikuwa zimefungwa, ghadhabu kubwa ikawaka ndani yao. 8 Wote walifanya shauri
pamoja, na walikuja kupigana dhidi ya Yerusalemu na kusababisha machafuko ndani
yake. 9 Lakini tuliomba kwa Mungu wetu na kuweka walinzi kama ulinzi dhidi
yao mchana na usiku kwa sababu ya tishio lao. 10 Kisha watu wa Yuda wakasema,
“Nguvu ya wale wanaobeba mizigo inashindwa. Kuna kifusi kikubwa, na hatuwezi
kujenga ukuta.” 11 Na adui zetu wakasema,” Wala hawatajua au kuona mpaka
tutakapokuja kati yao na kuwaua, na kuisimamisha kazi.” 12 Wakati huo Wayahudi
waliokuwa wakiishi karibu nao walitoka pande zote na kuzungumza nasi mara kumi,
wakituonya juu ya mipango waliyofanya dhidi yetu. 13 Kwa hiyo nikaweka watu
katika sehemu za chini za ukuta katika sehemu zilizo wazi. Niliweka kila familia
wenye upanga, mikuki, na upinde. 14 Nikatazama, nikasimama, nikawaambia wakuu,
na watawala, na watu wengine, “Msiogope. mkumbukeni Bwana, ambaye ni mkuu
na wa kushangaza. Wapiganie ndugu zenu, wana zenu, binti zenu, wake zenu na
nyumba zenu. 15 Ilipokuwa wakati adui zetu waliposikia kwamba mipango yao
ilikuwa inayojulikana kwetu, na Mungu alikuwa amebatilisha mipango yao, sote
tulirudi ukutani, kila mmoja kwa kazi yake. 16 Kwa hiyo tangu wakati huo nusu ya
watumishi wangu walifanya kazi tu juu ya kujenga ukuta, na nusu yao wakaishika
mikuki, ngao, pinde, na kuvaa silaha, wakati viongozi walisimama nyuma ya watu
wote wa Yuda. 17 Na hivyo wafanyakazi haohao ambao walikuwa wakijenga ukuta na
kubeba mizigo walikuwa pia wakilinda nafasi zao. Kila mtu alifanya kazi kwa mkono
mmoja, na kwa mkono mwingine alikuwa na silaha yake. 18 Kila mjenzi alivaa upanga
wake ubavuni mwake na ndivyo alivyojenga. Yule aliyepiga tarumbeta akakaa karibu
nami. 19 Niliwaambia wakuu na viongozi na watu wengine, “Kazi ni nzuri na ya kina,
na tumejitenga kwenye ukuta, mbali na mtu mwingine. 20 Lazima mkimbilie mahali
ambapo mtasikia sauti ya tarumbeta na kusanyika huko. Mungu wetu atatupigania.”
21 Kwa hiyo tulifanya kazi hiyo. Nusu yao walikuwa wakichukua mikuki kutoka
kupambazuka asubuhi hadi kutokea kwa nyota. 22 Nikawaambia watu wakati huo,
“Kila mtu na mtumishi wake waende usiku katikati ya Yerusalemu, ili wawe walinzi
wakati wa usiku na mfanyakazi wakati huo.” 23 Basi si mimi, wala ndugu zangu,
wala watumishi wangu, wala watu wa walinzi waliokuwa wananifuata, hakuna hata
mmoja wetu aliyebadili nguo zake, na kila mmoja wetu alichukua silaha yake, hata
kama angeenda kwa ajili ya kuteka maji.

# 5

1 Kisha wale wanaume na wake zao wakalia kwa nguvu dhidi ya Wayahudi wenzao.
2 Kwa maana kulikuwa na baadhi ya watu ambao walisema, “Sisi na wana wetu
na binti zetu tupo wengi. Basi hebu tupate nafaka tuweze kula na tukae tuishi.”
3 Pia kulikuwa na baadhi ya watu ambao walisema, “Tunaweka rehani mashamba
yetu, mizabibu yetu, na nyumba zetu ili tupate nafaka wakati wa njaa.” 4 Wengine
pia walisema, “Tumekopesha pesa kulipa kodi ya mfalme kwenye mashamba yetu
na mashamba yetu ya mizabibu. 5 Hata hivyo sasa miili yetu na damu ni sawa
na ndugu zetu, na watoto wetu ni sawa na watoto wao. Tunalazimishwa kuuza
wana wetu na binti zetu kuwa watumwa. Baadhi ya binti zetu tayari wamekuwa
watumwa. Lakini hatuna nguvu za kusaidia kwa sababu watu wengine sasa wana
mashamba yetu na mizabibu yetu.” 6 Nilikasirika sana niliposikia kilio chao na
maneno haya. 7 Kisha nikafikiri juu ya hili, na kuleta mashtaka dhidi ya wakuu
na viongozi. Nikawaambia, “Ninyi mnatafuta riba, kila mmoja kutoka kwa ndugu

yake mwenyewe.” Nikakutanisha kusanyiko kubwa juu yao [8] na kuwaambia, “Sisi,
kwa kadiri tulivyoweza, tumewakomboa toka utumwani ndugu zetu wa Kiyahudi
ambao walikuwa wameuzwa kwa mataifa, lakini hata mnawauza ndugu na dada
zenu ili wauzwe tena kwetu!” Walikuwa kimya na hawakupata neno la kusema. [9] Pia
nikasema, 'Mnachokifanya sio kizuri. Je, hampaswi kutembea katika hofu ya Mungu
wetu ili kuzuia malalamiko ya mataifa ambayo ni adui zetu? [10] Mimi na ndugu zangu
na watumishi wangu tunawapa fedha na nafaka. Lakini lazima tuache kutoza riba
juu ya mikopo hii. [11] Warudishieni leo leo mashamba yao, mizabibu yao, mashamba
yao ya mizeituni, na nyumba zao na asilimia ya fedha, nafaka, divai mpya, na mafuta
mliyowatoza.” [12] Wakasema, “Tutarudisha kile tulichochukua kutoka kwao, wala
hatutahitaji kitu kutoka kwao. Tutafanya kama unavyosema.” Ndipo nikawaita
makuhani, na kuwaapisha kuwafanya kama walivyoahidi. [13] Nikakung'uta vazi
langu, nikasema, “Basi Mungu aondoe nyumba na mali ya kila mtu asiyetimiza ahadi
yake. Kwa hiyo akung'utwe na kuwa hana kitu. Kusanyiko lote likasema “Amina,”
na wakamsifu Bwana. Na watu wakafanya kama walivyoahidi. [14] Kwa hiyo tangu
wakati niliowekwa kuwa mkuu wao katika nchi ya Yuda, tangu mwaka wa ishirini
mpaka mwaka wa thelathini na pili wa mfalme Artashasta, miaka kumi na miwili,
mimi na ndugu zangu hatukula chakula kilichotolewa kwa gavana. [15] Lakini wakuu
wa zamani waliokuwa kabla yangu waliwaweka watu mizigo mizito, na wakachukua
kwao shekeli arobaini za fedha kwa ajili ya chakula na divai yao ya kila siku. Hata
watumishi wao waliwadhulumu watu. Lakini sikufanya hivyo kwa sababu ya hofu
ya Mungu. [16] Niliendelea kufanya kazi kwenye ukuta, na hatukununua ardhi. Na
watumishi wangu wote walikusanyika huko kwa ajili ya kazi hiyo. [17] Katika meza
yangu walikuwa Wayahudi na maafisa, watu 150, isipokuwa wale waliokuja kwetu
kutoka kwa mataifa waliokuwa wakituzunguka. [18] Kila kitu kilichoandaliwa kila siku
kilikuwa ng'ombe moja, kondoo sita waliochaguliwa, na ndege, na kila siku kumi
aina zote za divai nyingi. Na hata kwa haya yote sikuhitaji mahitaji ya chakula cha
gavana, kwa sababu madai yalikuwa mazito sana juu ya watu. [19] Nikumbuke, Ee
Mungu wangu, kwa wema, kwa sababu ya yote niliyoyafanya kwa watu hawa.

# 6

[1] Wakati Sanbalati, Tobia, Geshemu Mwarabu na adui zetu wengine waliposikia
kwamba nilijenga upya ukuta na kwamba hakuna sehemu yoyote iliyoachwa ya
wazi, ingawa sijawaweka milango katika malango, [2] Sanbalati na Geshemu akatuma
wajumbe akasema, “Njoni, tukutane pamoja mahali fulani katika tambarare ya Ono.”
Lakini walitaka kunidhuru. [3] Niliwatuma wajumbe kwao, nikasema, “Ninafanya kazi
kubwa na siwezi kushuka. Kwa nini kazi isimame wakati nitakapoondoka na kuja
kwako?” [4] Walituma ujumbe huo huo mara nne, na mimi niliwajibu vile vile kila
wakati. [5] Sanbalati alimtuma mtumishi wake kwangu kwa njia ile ile mara ya tano,
na barua iliyo wazi mkononi mwake. [6] Imeandikwa, “Inaripotiwa kati ya mataifa,
na Geshemu pia anasema, kwamba wewe na Wayahudi mna mpango wa kuasi, kwa
sababu hiyo ndio mnajenga ukuta. Kutokana na taarifa hizi, unakaribia kuwa mfalme
wao. [7] Nawe umewachagua manabii kutangaza habari zako juu ya Yerusalemu,
wakisema, “Kuna mfalme huko Yuda!” Unaweza kuwa na hakika mfalme atasikia
ripoti hizi. Basi, hebu njoo tuzungumze. [8] Kisha nikamtuma neno nikisema, “mambo
kama hayo hayajafanyika kama unavyosema, kwa maana ndani ya moyo wako
umeyabuni.” [9] Kwa maana wote walitaka kututisha, wakifikiri, “Wataacha mikono
yao kufanya kazi hiyo, na haitafanyika.” Lakini sasa, Mungu, tafadhali imarisha
mikono yangu. [10] Nikaenda nyumbani kwa Shemaya mwana wa Delaya, mwana
wa Mehetabeli, aliyefungwa nyumbani mwake. Akasema, “Hebu tukutane pamoja

katika nyumba ya Mungu, ndani ya hekalu, na tufunge milango ya hekalu, kwa
maana wanakuja kukuua. Usiku wanakuja kukuua." [11] Nikajibu, "Je! Mtu kama mimi
ninaweza kukimbia? Na mtu kama mimi ninaweza kuingia hekaluni ili nipate kuishi?
Sitaingia." [12] Niligundua kwamba sio Mungu aliyemtuma, lakini alikuwa amefanya
unabii dhidi yangu. Tobia na Sanbalati walimwajiri. [13] Walimpa kazi kunifanya niwe
na hofu, ili nifanye kile alichosema na kutenda dhambi, hivyo wangeweza kunipa
jina baya ili kuniaibisha. [14] Mungu wangu, wakumbuke Tobia na Sanbalati, na yote
waliyofanya. Pia mkumbuke nabii Noadia na manabii wengine ambao walijaribu
kunifanya niogope. [15] Kwa hiyo ukuta ukamalizika siku ya ishirini na tano ya mwezi
wa Eluli, baada ya siku hamsini na mbili. [16] Adui zetu wote waliposikia hayo, mataifa
yote yaliyotuzunguka, waliogopa na wakakata tamaa sana machoni pao wenyewe.
Kwa maana walijua kazi hiyo ilifanyika kwa msaada wa Mungu wetu. [17] Wakati huu
wakuu wa Yuda walituma barua nyingi kwa Tobia, na barua za Tobia zikawajia.
[18] Kwa maana walikuwa wengi huko Yuda waliofungwa kwa kiapo chake, kwa
sababu alikuwa mkwewe Shekania, mwana wa Ara. Mwanawe Yehohanani alikuwa
amekuwa mkewe Meshulamu mwana wa Berekia. [19] Pia walizungumza nami kuhusu
matendo yake mema na kumwambia maneno yangu. Barua zililetwa kwangu kutoka
kwa Tobia kunitisha.

# 7

[1] Wakati ukuta ulipomalizika na milango nimekwisha kuisimamisha, na walinzi
wa malango na waimbaji na Walawi walikuwa wamechaguliwa, [2] nikampa ndugu
yangu Hanani kuwa na amri juu ya Yerusalemu, pamoja na Hanania ambaye alikuwa
msimamizi wa kijiji, kwa kuwa alikuwa mwaminifu na alimuogopa Mungu zaidi
kuliko wengi. [3] Nami nikawaambia, Msifungue malango ya Yerusalemu mpaka jua
litakapokuwa kali. Wakati walinzi wa mlango wanalinda, unaweza kufunga milango
na kuikaza. Chagua walinzi kutoka kwa wale wanaoishi Yerusalemu, wengine mahali
pa kituo chao cha ulinzi, na wengine mbele ya nyumba zao wenyewe. [4] Sasa jiji
lilikuwa pana na kubwa, lakini kulikuwa na watu wachache ndani yake, na hakuna
nyumba zilizojengwa tena. [5] Mungu wangu aliweka moyoni mwangu, kuwakusanya
pamoja wakuu, maafisa, na watu kuwaandikisha katika familia zao. Nilipata Kitabu
cha kizazi cha wale ambao walirudi kwanza na nikaona kwamba imeandikwa
humo. [6] Hawa ndio watu wa jimbo ambao walikwenda kutoka kwenye uhamisho wa
wale waliohamishwa ambao Nebukadreza mfalme wa Babeli aliwachukua mateka.
Wakarudi Yerusalemu na Yuda, kila mmoja kwenda kwenye mji wake. [7] Walikuja
na Zerubabeli, Yoshua, Nehemia, Seraya, Reelaya, Nahamani, Mordekai, Bilshani,
Mispari, Bigwai, Rehumu na Baana. Idadi ya wana wa Israeli ilikuwa. [8] Wana wa
Paroshi, 2, 172. [9] Wana wa Shefatia, 372. [10] Wana wa Ara, 652. [11] Wana wa Pahath
Moabu, [12] kwa wana wa Yeshua na Yoabu, 2, 818. [13] Wana wa Elamu, 1, 254. [14] Wana
wa Zatu, 845. Wana wa Zakai, 760. [15] Wana wa Binnui, 648. [16] Wana wa Bebai, 628.
[17] Wana wa Azgadi, 2, 322. [18] Wana wa Adonikamu, 667. [19] Wana wa Bigwai, 2, 067.
[20] Wana wa Adini, 655. [21] Wana wa Ateri, wa Hezekia, 98. [22] Wana wa Hashumu, 328.
[23] Wana wa Besai, 324. [24] Wana wa Harifu, 112. [25] Wana wa Gibeoni, 95. [26] Watu
kutoka Bethlehemu na Netofa, 188. [27] Watu wa Anathothi, 128. [28] Watu wa Beth
Azmaweth, 42. [29] Watu wa Kiriath Yearimu, Kefira, na Beerothi, 743. [30] Watu wa
Rama na Geba, 621. [31] Watu wa Mikmasi, 122. [32] Watu wa Betheli na Ai, 123. [33] Watu
wa Nebo, 52. [34] Watu wa Elamu wa pili, 1, 254. [35] Watu wa Harimu, 320. [36] Watu
wa Yeriko, 345. [37] Watu wa Lodi, Hadidi, na Ono, 721. [38] Watu wa Senaa, 3, 930.
[39] makuhani Wana wa Yedaya (wa nyumba ya Yeshua), 973. [40] Wana wa Imeri, 1,
052. [41] Wana wa Pashuri, 1, 247. [42] Wana wa Harimu, 1, 017. [43] Walawi, wana wa
Yeshua, wa Kadmieli, wa Binui, wa Hodavia, 74. [44] Waimbaji wana wa Asafu; 148.

45 Waliofungua mlango wana wa Shalumu, wana wa Ateri, wana wa Talmoni; wana
wa Akubu, wana wa Hatita, wana wa Shobai, 138. 46 Watumishi wa Hekalu wana wa
Siha, wana wa Hasufa, wana wa Tabaothi, 47 wana wa Kerosi, wana wa Siaha, wana
wa Padoni, 48 wana wa Lebana, wana wa Hagaba, wana wa Salmai, 49 wana wa wa
Hanani, wana wa Gideli, wana wa Gahari. 50 Wana wa Reaya, wana wa Resini, wana
wa Nekoda, 51 wana wa Gazamu, wana wa Uza, wana wa Pasea, 52 wana wa Besai,
wana wa Meunimu, wana wa Nefusimu. 53 Wana wa Bakbuki, wana wa Hakufa,
wana wa Harhuri, 54 wana wa Baslith, wana wa Mehida, wana wa Harsha, 55 wana wa
Barkosi, wana wa Sisera, wana wa Tema, 56 wana wa Nesia, wana wa Hatifa. 57 Wana
wa Sulemani, wana wa Sotai, wana wa Sofeereth, wana wa Peruda, 58 wana wa Yaala,
wana wa Darkoni, wana wa Gideli, 59 wana wa Shefatia, wana wa Hatili, wana wa
Pokerethi Sebaimu, wana wa Amoni. 60 Watumishi wote wa hekalu, na wana wa
watumishi wa Sulemani, walikuwa 392. 61 Hawa ndio watu waliokwenda kutoka Tel
Mela, Tel harsha, Kerub, Addon, na Imeri. Lakini hawakuweza kuthibitisha kwamba
wao au jamaa za baba zao walikuwa wana wa Israeli, 62 wana wa Delaya, wana wa
Tobia, na wana wa Nekoda, 642. 63 Na kutoka kwa makuhani Wana wa Habaya,
Hakosi, na Barzilai ( akamchukua mkewe kutoka kwa binti za Barzilai wa Gileadi na
akaitwa kwa jina lao). 64 Hawa walitafuta rekodi zao kati ya waliojiunga na kizazi
chao, lakini hawakuweza kupatikana, kwa hivyo waliondolewa katika ukuhani kama
walio najisi. 65 Naye mkuu wa gavana akawaambia wasiruhusiwe kula chakula cha
makuhani kutoka kwenye dhabihu mpaka atakapoinuka kuhani mwenye Urimu na
Thumimu. 66 Kusanyiko lote lilikuwa 42, 360, 67 isipokuwa watumishi wao wa kiume
na watumishi wao wa kike, ambao walikuwa 7, 337. Walikuwa na wanaume na
wanawake wa kuimba 245. 68 Farasi zao zilikuwa 736 kwa idadi, nyumbu zao, 245,
69 ngamia zao, 435, na punda zao, 6, 720. 70 Baadhi ya wakuu wa familia za baba zao
walitoa zawadi kwa ajili ya kazi. Gavana alitoa sadaka ya darkoni elfu ya dhahabu,
mabakuli 50, na mavazi 530 ya makuhani. 71 Baadhi ya wakuu wa familia za baba zao
waliwapa katika hazina kwa kazi darkroni elfu ishirini za dhahabu na mane 2, 200 za
fedha. 72 Watu wengine waliwapa darkoni za dhahabu ishirini elfu, na dhahabu elfu
mbili za fedha, na mavazi sitini na saba kwa makuhani. 73 Basi makuhani, Walawi,
walinzi wa malango, waimbaji, watu wengine, watumishi wa hekalu, na Israeli wote
waliishi katika miji yao. Hata mwezi wa saba watu wa Israeli walikuwa wakiishi
katika miji yao."

# 8

1 Watu wote walikusanyika kama mtu mmoja katika eneo la wazi mbele ya lango
la maji. Wakamwomba Ezra mwandishi akilete Kitabu cha Sheria ya Musa, ambacho
Bwana aliwaamuru Israeli. 2 Siku ya kwanza ya mwezi wa saba, Ezra, kuhani,
akaleta sheria mbele ya mkutano, wanaume na wanawake, na wote waliokuwa
na uwezo wa kusikia na kuelewa. 3 Akatizama eneo lililo wazi mbele ya lango la
Maji, na akasoma toka asubuhi hadi adhuhuri, mbele ya wanaume na wanawake,
na yeyote ambaye angeweza kuelewa. Na wote wakasikiliza kwa makini kitabu
cha Sheria. 4 Na Ezra, mwandishi, alisimama juu ya jukwaa la mbao ambalo watu
walikuwa wametengeneza kwa kusudi hilo. Pembeni yake walisimama Matithia,
Shema, Anaya, Uria, Hilkia na Maaseya, upande wake wa kuume; na Pedaya, Misbaeli,
Malkiya, Hashumu, Hashbadani, Zekaria na Meshulamu walikuwa wamesimama
upande wake wa kushoto. 5 Ezra alifungua kitabu mbele ya watu wote, kwa kuwa
alikuwa amesimama juu ya watu, na alipoufungua watu wote wakasimama. 6 Ezra
akamshukuru Bwana, Mungu mkuu; na watu wote wakainua mikono yao, wakajibu,
"Amina! Amina!" Wakainamisha vichwa vyao, wakamwabudu Bwana kwa nyuso
zao zikiwa chini. 7 Yeshua, Bani, Sherebia, Yamini, Akubu, Shabethai, Hodai,

Maaseya, Kelita, Azaria, Yozabidi, Hanania, Pelaya nao ni Walawi, waliwasaidia watu
kuelewa sheria, watu wakakaa mahali pao. 8 Wao walisoma katika kitabu, Sheria ya
Mungu, wakaeleza wazi kwa tafsiri na kutoa maana ili watu waelewe yaliyosomwa.
9 Nehemia, gavana, na Ezra kuhani, na mwandishi, na Walawi waliokuwa wakitafsiri
kwa watu, wakawaambia watu wote, Siku hii ni takatifu kwa Bwana, Mungu wenu.
Msiomboleze au kulia. Kwa kuwa watu wote walilia wakati waliposikia maneno
ya sheria. 10 Nehemia akawaambia, 'Nendeni, mle kilichonona, mkate na maji
ya kunywa, na mpelekeni mtu asiye na kitu, kwa maana siku hii ni takatifu kwa
Bwana wetu. Msiwe na huzuni, kwa kuwa furaha ya Bwana ni nguvu zenu. 11 Basi
Walawi wakawafanya watu kuwa na utulivu, wakisema, “Nyamazeni! kwa maana
siku hii ni takatifu. Msiwe na huzuni.” 12 Watu wote wakaenda kula na kunywa
na kugawana chakula na kusherehekea kwa furaha kubwa kwa sababu walielewa
maneno waliyohubiriwa. 13 Siku ya pili viongozi wa nyumba za mababu kutoka
kwa watu wote, makuhani na Walawi, wakakusanyika kwa Ezra, mwandishi ili
kupata ufahamu kutoka kwenye maneno ya sheria. 14 Wakaona imeandikwa katika
sheria namna Bwana alivyomuamuru Musa kwamba wana wa Israeli waishi katika
hema wakati wa sikukuu ya mwezi wa saba. 15 Wanapaswa kutoa tamko katika
miji yao yote, na huko Yerusalemu, wakisema, 'Nendeni nje kwenye nchi ya vilima,
na mkalete matawi kutoka kwenye mzeituni mwitu, na matawi ya mihadsi, na
matawi ya mitende na matawi ya miti minene ili kufanya vibanda vya muda kama
ilivyoandikwa.” 16 Basi watu wakatoka na kuleta matawi, wakajifanyia mahema, kila
mmoja juu ya paa zao, katika ua zao, katika mahakama za nyumba ya Mungu, mahali
pa wazi pa lango la Maji, na katika mraba wa lango la Efraimu. 17 Kisha kusanyiko
lote la wale waliorudi kutoka kifungoni wakafanya mahema na kukaa ndani yake.
Kwa kuwa tangu siku za Yoshua, mwana wa Nuni hata siku hiyo, watu wa Israeli
hawakuadhimisha sikukuu hii. Na furaha ilikuwa kubwa sana. 18 Pia siku kwa siku,
tangu siku ya kwanza hadi mwisho, Ezra alisoma kutoka Kitabu cha Sheria ya Mungu.
Walifanya sikukuu kwa siku saba na siku ya nane kilikuwa na kusanyiko zuri, kwa
utiifu wa amri.

# 9

1 Siku ya ishirini na nne ya mwezi huo huo watu wa Israeli walikusanyika, nao
walikuwa wamefunga, nao walikuwa wamevaa magunia, nao wakaweka vumbi juu
ya vichwa vyao. 2 Wazao wa Israeli walijitenga na wageni wote. Walisimama na
kukiri dhambi zao wenyewe na matendo maovu ya baba zao. 3 Walisimama mahali
pao, na robo ya siku walisoma kutoka Kitabu cha Sheria ya Bwana Mungu wao. Na
robo nyingine ya siku walikiri na kuinama mbele ya Bwana Mungu wao. 4 Walawi,
Yeshua, Bani, Kadmieli, Shebaniya, Buni, Sherebia, Bani na Kenani, walisimama juu
ya ngazi, wakamwita Bwana, Mungu wao kwa sauti kubwa. 5 Ndipo Walawi, na
Yeshua, na Kadmieli, na Bani, na Hashabneya, na Sherebia, na Hodia, na Shebania, na
Pethalia, wakasema, “Simameni, mkamsifu Bwana, Mungu wenu, milele na milele.”
“Libarikiwe jina lako tukufu, lililotukuka kuliko baraka zote na sifa zote. 6 Wewe ni
Bwana. Wewe peke yako. Wewe umefanya mbinguni, mbingu za juu, na malaika
wote wa vita vita, na dunia na kila kitu kilicho juu yake, na bahari na vyote
vilivyomo. Unawapa wote uzima, na majeshi ya malaika wanakusujudia. 7 Wewe
ndiwe Bwana, Mungu aliyemchagua Abramu, akamtoa kutoka Uri wa Wakaldayo,
akamwita Ibrahimu. 8 Uliona moyo wake ulikuwa mkamilifu mbele yako, nawe
ukafanya pamoja naye agano la kuwapa wazao wake nchi ya Wakanaani, na Mhiti,
na Mwamori, na Perizi, na Myebusi, na Wagirgashi. Umeweka ahadi yako kwa
sababu wewe ni mwenye haki. 9 Uliona shida ya baba zetu Misri na ukasikia kilio

chao kando ya bahari ya shamu. [10] Wewe ulifanya ishara na maajabu juu ya Farao,
na watumishi wake wote, na watu wote wa nchi yake, kwa maana ulijua kwamba
Wamisri walifanya kwa kujivunia. Lakini ulijifanyia jina ambalo linasimama hadi
siku leo. [11] Ukagawanya bahari mbele yao, wakavuka katikati ya bahari juu ya nchi
kavu; na ukawatupa wale waliowa ndani ya kina, kama jiwe ndani ya maji ya kina.
[12] Wewe uliwaongoza kwa nguzo ya wingu wakati wa mchana, na kwa nguzo ya
moto wakati wa usiku, ili kuwamulikia njiani waweze kutembea katika nuru yake.
[13] Ulishuka juu ya Mlima Sinai ukazungumza nao kutoka mbinguni ukawapa amri
za haki na sheria za kweli, amri nzuri na maagizo. [14] Uliwajulisha sabato yako
takatifu, ukawapa amri, maagizo, na sheria kupitia Musa mtumishi wako. [15] Uliwapa
chakula kutoka mbinguni kwa ajili ya njaa yao, na maji kutoka mwamba kwa kiu
yao, ukawaambia waende kuimiliki nchi uliyowaapa kwa kiapo kuwapa. [16] Lakini
wao na baba zetu walifanya uasi, nao walikuwa wakaidi, wala hawakuzitii amri
zako. [17] Walikataa kusikiliza, na hawakufikiri juu ya maajabu uliyofanya kati yao,
lakini wakawa wakaidi, na katika uasi wao waliweka kiongozi ili wairudie hali ya
utumwa. Lakini wewe ni Mungu ambaye amejaa msamaha, mwenye rehema na
huruma, si mwepesi wa hasira, na wingi katika upendo thabiti. Wewe haukuwaacha.
[18] Wala hukuwaacha hata walipokwisha kutoa ndama katika chuma kilichochomwa
na kusema, "Huyu ndio Mungu wenu aliyekuleta kutoka Misri," wakati walipopotoka
sana. [19] Wewe, kwa huruma yako, hukuwaacha katika jangwa. Nguzo ya wingu
iliyowangoza njiani haikuwaacha wakati wa mchana, wala nguzo ya moto usiku
iliwaangazia barabara ambayo walipaswa kutembea. [20] Uliwapa Roho wako mzuri
kuwafundisha, na mana yako haukuwanyima kinywani mwao, na ukawapa maji kwa
kiu yao. [21] Kwa miaka arobaini uliwaruzuku jangwani, na hawakukosa chochote.
Nguo zao hazikuchakaa na miguu yao haikuvimba. [22] Uliwapa falme na watu, na
ukawapa ardhi katika kila kona ya mbali. Basi wakaimiliki nchi ya Sihoni mfalme
wa Heshboni, na nchi ya Ogu mfalme wa Bashani. [23] Uliwafanya watoto wao kuwa
wengi kama nyota za mbinguni, na ukawaingiza katika nchi. Uliwaambia baba zao
waingie na kumiliki. [24] Basi watu wakaingia, wakaimiliki nchi, ukawashinda wenyeji
wa nchi hiyo, Wakanaani. Ukawatia mikononi mwao, pamoja na wafalme wao na
watu wa nchi, ili Israeli afanye nao kama walivyotaka. [25] Wao waliteka miji yenye
nguvu na nchi yenye ustawi, nao wakachukua nyumba zenye vitu vyote vyema, birika
zilizochimbwa, mizabibu na miti ya mizeituni, na miti ya matunda mengi. Kwa hiyo
walikula na wakashiba na wakatosheka, na wakafurahi kwa wema wako. [26] Basi
hawakukutii na wakawaasi. Walitupa sheria yako nyuma ya migongo yao. Waliwaua
manabii wako waliowaonya wakurudie wewe, nao wakafanya ukatili mkubwa.
[27] Kwa hiyo ukawatia mikononi mwa adui zao, aliyewatesa. Na wakati wa mateso
yao, walikulilia na wewe uliwasikia kutoka mbinguni na mara nyingi ukawaokoa
katika mikono ya adui zao, kwa sababu ya huruma zako nyingi. [28] Lakini baada ya
kupumzika, wakafanya mabaya tena mbele yako, nawe ukawaacha mikononi mwa
adui zao, kwa hiyo adui zao wakatawala juu yao. Hata walipokurudia na kukulilia,
ukasikia kutoka mbinguni, mara nyingi ukawaokoa kwa sababu ya huruma yako.
[29] Uliwaonya ili wapate kurudi kwenye sheria yako. Hata hivyo walifanya kiburi na
hawakusikiliza amri zako. Walifanya dhambi dhidi ya amri zako ambazo humpa
uzima mtu yeyote anayezitii. Hawakuzitii, hawakuzitenda na walikataa kuzisikiliza.
[30] Kwa miaka mingi ukachukiliana nao na kuwaonya kwa Roho wako kwa njia ya
manabii wako. Hata hivyo hawakusikiliza. Kwa hiyo ukawatia mikononi mwa watu
wa jirani. [31] Lakini kwa huruma zako kubwa hukuwakomesha kabisa, au kuwaacha,
kwa maana wewe ni Mungu mwenye rehema na mwenye huruma. [32] Basi, Mungu
wetu, Mungu wetu mkuu, mwenye nguvu na mwenye kutisha, unayeweka agano

lako na upendo wako, shida zote zilizotupata sisi, wafalme wetu, wakuu wetu, na
makuhani wetu, na manabii wetu, na baba zetu, na watu wako wote tangu siku za
wafalme wa Ashuru mpaka leo usizihesabu kuwa ni kidogo. 33 Wewe ni mwenye
haki katika yote yaliyotupata, kwa kuwa umetenda kwa uaminifu, na tumefanya
uovu. 34 Wafalme wetu, wakuu wetu, makuhani wetu, na baba zetu hawakuishika
sheria yako, wala hawakuzingatia amri zako au shuhuda zako ulizowashuhudia.
35 Hata katika ufalme wao wenyewe, wakati walifurahia wema wako kwao, katika
nchi kubwa na yenye mazao uliyoweka mbele yao, hawakukutumikia au kuacha
njia zao mbaya. 36 Sasa sisi ni watumwa katika nchi uliyowapa baba zetu kufurahia
matunda yake na zawadi zake nzuri, na tazama, sisi ni watumwa! 37 Mavuno mazuri
kutoka nchi yetu huenda kwa wafalme uliowaweka juu yetu kwa sababu ya dhambi
zetu. Watawala juu ya miili yetu na juu ya mifugo kama wanavyopenda. Tuna shida
kubwa. 38 Kwa sababu ya yote haya, tunafanya agano thabiti kwa kuandika. Kwenye
hati iliyofungwa ni majina ya wakuu wetu, Walawi, na makuhani.”

# 10

1 Wale ambao waliweka majina yao kwenye nyaraka zilizofunikwa walikuwa
Nehemia mwana wa Hakalia gavana, na makuhani waliowekwa walikuwa Sedekia,
2 Seraya, Azaria, Yeremia, 3 Pashuri, Amaria, Malkiya, 4 Hamshi, Shekania, Maluki,
5 Harimu, Meremothi, Obadia, 6 Danieli, Ginethoni, Baruki, 7 Meshulamu, Abiya,
Miyamini, 8 Maazia, Bilgai na Shemaya. Hawa walikuwa makuhani. 9 Walawi
walikuwa Yeshua mwana wa Azania, Binui wa jamaa ya Henadadi, Kadmieli,
10 na Walawi wenzake, Shebania, Hodia, Kelita, Pelaya, Hanani, 11 Mika, Rehobu,
Hashabia, 12 Zakuri, Sherebia, Shebania, 13 Hodiya, Bani na Beninu. 14 Viongozi wa
watu walikuwa Paroshi, Pahath-Moabu, Elamu, Zatu, Bani, 15 Buni, Azgadi, Bebai,
16 Adoniya, Bigwai, Adini, 17 Ateri, Hezekia, Azuri, 18 Hodia, Hashumu, Besai, 19 Harifu,
Anathothi, Nobai, 20 Magpiashi, Meshulamu, Heziri, 21 Meshezabeli, Sadoki, Yadua,
22 Pelatia, Hanani, AnaYA, 23 Hoshea, Hanania, Hashubu, 24 Haloheshi, Pilha, Shobeki,
25 Rehumu, Hashabna, Maaseya, 26 Ahia, Hanani, Anani, 27 Maluki, Harimu na Baana.
28 Na watu wengine waliokuwa makuhani, na Walawi, na walinzi wa malango, na
waimbaji, na watumishi wa hekalu, na wote waliokuwa wamejitenga wenyewe na
watu wa nchi za jirani, kwa sheria ya Mungu, na wanawake zao, na wana wao,
na Binti zao, wote walio na ujuzi na ufahamu, 29 walijiunga na ndugu zao, wakuu
wao, na kujifunga katika laana na kiapo cha kutembea katika sheria ya Mungu,
iliyotolewa na Musa mtumishi wa Mungu, na kuzingatia na kutii amri zote za Bwana
Mungu wetu na hukumu zake na sheria zake. 30 Tuliahidi kuwa hatuwezi kuwapa
binti zetu watu wa nchi au kuchukua binti zao kwa wana wetu. 31 Pia tuliahidi
kwamba ikiwa watu wa nchi wataleta bidhaa au nafaka yoyote ya kuuza siku ya
Sabato, hatuwezi kununua kutoka kwao siku ya Sabato au siku yoyote takatifu.
Kila mwaka wa saba tutaacha mashamba yetu kupumzika, na tutafuta madeni yote
yaliyotokana na Wayahudi wengine. 32 Tulikubali amri za kutoa shilingi ya shekeli
kila mwaka kwa ajili ya huduma ya nyumba ya Mungu wetu, 33 kutoa mkate wa
uwepo, na sadaka ya nafaka ya kawaida, sadaka za kuteketezwa siku za Sabato,
sikukuu mpya za mwezi na sikukuu za kuteketezwa, na sadaka takatifu, na sadaka
za dhambi za kufanya upatanisho kwa Israeli, pamoja na kazi yote ya nyumba ya
Mungu wetu. 34 Na makuhani, Walawi, na watu wakapiga kura kwa ajili ya sadaka
ya kuni. Kura ilichagua ni nani wa familia zetu ataleta kuni ndani ya nyumba ya
Mungu wetu kwa nyakati zilizowekwa kila mwaka. Kuni hizo zilichomwa juu ya
madhabahu ya Bwana Mungu wetu, kama ilivyoandikwa katika sheria. 35 Tuliahidi
kuleta nyumbani kwa Bwana matunda ya kwanza yaliyotokana na udongo wetu, na

matunda ya kwanza ya mti kila mwaka. [36] Na kama ilivyoandikwa katika sheria,
tuliahidi kuleta nyumbani kwa Mungu na kwa makuhani watumikao hapo wazaliwa
wa kwanza wa wana wetu ma wanyama wetu. [37] Tutaleta unga wa kwanza na
sadaka zetu za nafaka, na matunda ya kila mti, na divai mpya na mafuta tutaleta kwa
makuhani, kwenye vyumba vya kuhifadhi vya nyumba ya Mungu wetu. Tutawaletea
Walawi sehemu ya kumi kutoka kwenye udongo wetu kwa sababu Walawi hukusanya
zaka katika miji yote tunayofanya kazi. [38] Kuhani, mzao wa Haruni, lazima awe na
Walawi wakati wanapopokea zaka. Walawi wanapaswa kuleta sehemu ya kumi ya
zaka katika nyumba ya Mungu wetu kwenye vyumba vya kuhifadhi hazima. [39] Kwa
maana wana wa Israeli na wana wa Lawi, wataleta sadaka za nafaka, divai mpya, na
mafuta katika vyumba vya kuhifadhi ambapo vitu vya patakatifu vinasimamishwa,
na mahali pa makuhani watumishi, na walinzi wa mlango, na waimbaji. Hatuwezi
kuacha nyumba ya Mungu wetu.

# 11

[1] Viongozi wa watu waliishi Yerusalemu, na watu wengine walipiga kura ili
kuleta mmoja kati ya watu kumi kuishi Yerusalemu, mji mtakatifu, na wengine
tisa walibakia katika miji mingine. [2] Na watu wakawabariki wote waliojitoa kwa
hiari kuishi Yerusalemu. [3] Hawa ndio viongozi wa mkoa ambao waliishi Yerusalemu.
Hata hivyo, katika miji ya Yuda kila mtu aliishi katika nchi yake mwenyewe, ikiwa
ni pamoja na Waisraeli, makuhani, Walawi, watumishi wa hekalu, na wazao wa
watumishi wa Sulemani. [4] Katika Yerusalemu waliishi baadhi ya wana wa Yuda na
baadhi ya wana wa Benyamini. Watu wa Yuda walikuwa pamoja na Athaya, mwana
wa Uzia, mwana wa Zekaria, mwana wa Amaria, mwana wa Shefatia, mwana wa
Mahalaleli, mwana wa Peresi. [5] Na Maaseya, mwana wa Baruki, mwana wa Kolhoze,
mwana wa Hazaya, mwana wa Adaya, mwana wa Yoyaribu, mwana wa Zakaria,
mwana wa Mshelani, alikuwa mwana wa Baruki. [6] Wana wote wa Peresi waliokaa
Yerusalemu walikuwa 468. Walikuwa masujaa. [7] Hao ndio wana wa Benyamini, Salu,
mwana wa Meshulamu, mwana wa Yoedi, mwana wa Pedaya, mwana wa Kolaya,
mwana wa Maaseva, mwana wa Ithieli, mwana wa Yehaya. [8] Na baada yake, Gabai na
Salai, watu 928. [9] Yoeli mwana wa Zikri alikuwa mwangalizi wao; na Yuda mwana wa
Hasenua alikuwa mkuu wa pili juu ya mji. [10] Kutoka kwa makuhani Yedaya, mwana
wa Yoyaribu, Yakini, [11] Seraya mwana wa Hilikia, mwana wa Meshulamu, mwana
wa Sadoki, mwana wa Merayoti, mwana wa Ahitubu, mkuu wa nyumba ya Mungu,
[12] na wenzake waliofanya kazi ya ukoo, watu 822. na Adaya mwana wa Yerohamu,
mwana wa Pelalia, mwana wa Amzi, mwana wa Zekaria, mwana wa Pashuri, mwana
wa Malkiya. [13] Nao walikuwa washirika wake waliokuwa wakuu wa jamaa, wanaume
242, na Maasai mwana wa Azareli, mwana wa Azai, mwana wa Meshilemothi, mwana
wa Imeri; [14] na ndugu zao, 128 wapiganaji wenye ujasiri, wenye ujasiri; Waziri wao
aliyeongoza alikuwa Zabdieli, mwana wa Hageoli. [15] Na Walawi Shemaya mwana
wa Hashubu, mwana wa Azrikamu, mwana wa Hashabia, mwana wa Buni, [16] na
Shabethai, na Yozabadi, ambao walikuwa ni viongozi wa Walawi, waliosimamia kazi
za nje ya nyumba ya Mungu. [17] Alikuwepo Matania, mwana wa Mika, mwana wa
Zakri, mwana wa Asafu, aliyekuwa mkurugenzi aliyeanza shukrani kwa sala, na
Bakbukia, wa pili miongoni mwa ndugu zake, na Abda mwana wa Shemaya, mwana
wa Galali, mwana wa Yeduthuni. [18] Katika mji wote mtakatifu walikuwa Walawi
284. [19] Walinzi wa malango Akubu, Talmoni, na washirika wao, ambao waliolinda
milango, wanaume 172. [20] Na wale waliosalia wa Israeli, na makuhani, na Walawi,
walikuwa katika miji yote ya Yuda. Kila mtu aliishi katika milki yake mwenyewe.
[21] Wafanyakazi wa hekalu waliishi Ofeli, na Siha na Gishpa walikuwa wakiwaongoza.

[22] Mtawala mkuu juu ya Walawi waliokuwa wakitumikia Yerusalemu alikuwa Uzi
mwana wa Bani, mwana wa Hashabia, mwana wa Matania, mwana wa Mika, wa
wana wa Asafu, ambao walikuwa waimbaji wa kazi katika nyumba ya Mungu.
[23] Walikuwa chini ya maagizo kutoka kwa mfalme na maagizo imara yalitolewa
kwa waimbaji kila siku inavyohitajika. [24] Pethahia mwana wa Meshezabeli, mwana
wa Zera, mwana wa Yuda, alikuwa upande wa mfalme kwa habari zote za watu.
[25] Kuhusu vijiji na mashamba yao, baadhi ya watu wa Yuda wakakaa Kiriath-arba,
na vijiji vyake, na Diboni, na vijiji vyake, na Yekabzeeli na vijiji vyake. [26] Wakaishi
katika Yeshua, Molada, Beth-Peleti, [27] Hazar-Shuali, Beersheba na vijiji vyake. [28] Nao
wakakaa Siklagi, na Mekona, na vijiji vyake, [29] Enrimoni, Sora, Yarmuthi, [30] Zanoa,
Adulamu, na vijiji vyake, na Lakishi, na mashamba yake, na Azeka, na vijiji vyake.
Basi wakakaa kutoka Beer-sheba mpaka bonde la Hinomu. [31] Watu wa Benyamini
pia walikuwa wakiishi kutoka Geba, kwenda Mikmashi na Aiya, na Beth-eli na vijiji
vyake. [32] Waliishi Anathothi, Nobu, Anania, [33] Hazori, Rama, Gitaimu, [34] Hadidi,
Seboimu, Nebalati, [35] Lodi, na Ono, bonde la wafundi. [36] Walawi wengine waliishi
Yuda wengine Benyamini.

# 12

[1] Hawa ndio makuhani na Walawi waliokuja pamoja na Zerubabeli mwana wa
Shealueli, pamoja na Yoshua Seraya, Yeremia, Ezra, [2] Amaria, Maluki, Hatushi,
[3] Shekania, Harimu na Meremothi. [4] Kulikuwa na Iddo, Ginethoni, Abiya, [5] Miyamini,
Maazia, Bilgai, [6] Shemaya, Yoyaribu, Yedaya, [7] Salu, Amoki, Hilkia, na Yedaya.
Hawa walikuwa wakuu wa makuhani na washirika wao katika siku za Yoshua.
[8] Walawi walikuwa Yeshua, Binui, Kadmieli, Sherebia, Yuda, na Matania, aliyekuwa
akiongoza nyimbo za shukrani, pamoja na washirika wake. [9] Bakbukia na Uno,
washirika wao, walisimama pembeni yao wakati wa huduma. [10] Yoshua alikuwa
babaye Yoyakimu, Yoyakimu alikuwa baba wa Eliashibu, Eliashibu alikuwa babaye
Yoyada, [11] Yoyada alimzaa Yonathani, Yonathani akamzaa Yadua. [12] Katika siku za
Yoyakimu hawa walikuwa makuhani, wakuu wa jamaa; Meraya alikuwa mkuu wa
Seraya, Hanania alikuwa kiongozi wa Yeremia, [13] Meshulam alikuwa kiongozi wa
Ezra, Yehohanani alikuwa kiongozi wa Amaria, [14] Yonathani alikuwa kiongozi wa
Maluki, na Yusufu alikuwa kiongozi wa Shekania. [15] Ili kuendelea, Adna alikuwa
kiongozi wa Harimu, Helkai kiongozi wa Meremothi, [16] Zekaria alikuwa kiongozi
wa Ido, Meshulamu alikuwa kiongozi wa Ginethoni, na [17] Zikri alikuwa kiongozi
wa Abia wa Miyaamini. Piltai alikuwa kiongozi wa Maazia. [18] Shamua alikuwa
kiongozi wa Bilgai, Yehonathani alikuwa kiongozi wa Shemaya, [19] Matenai alikuwa
kiongozi wa Yoyaribu, Uzi alikuwa kiongozi wa Yedaya, [20] Kalai alikuwa kiongozi
wa Salu, Eberi alikuwa kiongozi wa Amok, [21] Hashabia alikuwa kiongozi wa Hilkia,
na Nethanel alikuwa kiongozi wa Yedaya. [22] Katika siku za Eliashibu, Walawi
Eliashibu, Yoyada, Yohana, na Yadua waliandikwa kama vichwa vya familia, na
makuhani waliandikwa wakati wa utawala wa Dariyo wa Persia. [23] Wana wa Lawi
na viongozi wao wa familia waliandikwa katika Kitabu cha tarehe hadi siku za
Yohana mwana wa Eliashibu. [24] Wakuu wa Walawi walikuwa Hashabia, Sherebia,
na Yeshua mwana wa Kadmieli, pamoja na washirika wao, waliokuwa wamesimama
mbele yao kumtukuza na kumshukuru, akijibu sehemu kwa sehemu, kwa kutii amri
ya Daudi, mtu wa Mungu. [25] Matania, Bakbukia, Obadiya, Meshulamu, Talmoni
na Akubu walikuwa walinzi wa malango waliokuwa wakiwa wamesimama katika
vyumba vya hazina penye malango. [26] Walitumika katika siku za Yoyakimu, mwana
wa Yoshua, mwana wa Yosadaki, na katika siku za Nehemiya, gavana na Ezra kuhani
na mwandishi. [27] Katika kujitolea kwa ukuta wa Yerusalemu, watu walitafuta Walawi

popote walipokuwa wakiishi, wakawaleta Yerusalemu ili kusherehekea kujitolea kwa
furaha, pamoja na shukrani na kuimba kwa ngoma, vinanda na vinubi. 28 Ushirika
wa waimbaji walikusanyika pamoja kutoka wilaya iliyozunguka Yerusalemu na
kutoka vijiji vya Wanetofathi. 29 Walikuja kutoka Beth-gilgali na kutoka katika
mashamba ya Geba na Azmawethi, kwa kuwa waimbaji walikuwa wamejijengea vijiji
karibu na Yerusalemu. 30 Makuhani na Walawi wakajitakasa, kisha wakawatakasa
watu, milango na ukuta. 31 Kisha nilikuwa na viongozi wa Yuda kwenda juu ya
ukuta, na mimi kuteua mikutano miwili mikubwa ya hao walioshukuru. Mmoja
alienda upande wa kulia juu ya ukuta kuelekea lango la jaa. 32 Hoshaya na nusu ya
viongozi wa Yuda walimfuata, 33 na baada yake akaenda Azaria, Ezra na Meshulamu,
34 Yuda, Benyamini, Shemaya, Yeremia 35 na wana wa makuhani waliokuwa na
tarumbeta, na Zekaria mwana wa Yonathani, mwana wa Shemaya, mwana wa
Mataniya, mwana wa Mikaya, mwana wa Zakuri, mwana wa Asafu. 36 Na pia jamaa
za Zekaria, Shemaya, Azareli, Milalai, Gilalai, Maai, Nethaneli, Yuda, Hanani, pamoja
na vyombo vya muziki vya Daudi mtu wa Mungu. Ezra mwandishi alikuwa mbele
yao. 37 Na kwa Lango la Chemchemi walikwenda moja kwa moja na madaraja ya
mji wa Daudi juu ya kupanda kwa ukuta, juu ya nyumba ya Daudi, kwenye lango la
Maji upande wa mashariki. 38 Na waimbaji wengine ambao walishukuru wakaenda
upande mwingine. Niliwafuata juu ya ukuta pamoja na nusu ya watu, juu ya mnara
wa vinyago, hadi kuta kubwa, 39 na juu ya lango la Efraimu, na mlango wa kale,
na kwa lango la samaki na mnara wa Hananeli na mnara wa Hamea, kwa lango la
Kondoo, na wakasimama kwenye mlango wa walinzi. 40 Kwa hiyo, mikutano miwili
ya wale waliomshukuru walipata nafasi yao katika nyumba ya Mungu, na mimi
pia nikachukua nafasi yangu na nusu ya viongozi pamoja nami. 41 Na makuhani
wakachukua nafasi zao Eliakimu, Maaseya, Miyamini, Mikaya, Elioenai, Zekaria,
na Hanania wenye tarumbeta, 42 Maaseya, na Shemaya, Eleazari, Uzi, Yehohanani,
Malkiya, Elamu, Ezeri. Waimbaji waliimba na Yezrahia kama wasimamizi. 43 Walitoa
dhabihu kubwa siku ile, wakafurahi, kwa sababu Mungu alikuwa amewafurahisha
kwa furaha kubwa. Pia wanawake na watoto walifurahi. Hivyo furaha ya Yerusalemu
ikasikiwa toka mbali. 44 Siku hiyo watu waliteuliwa juu ya nyumba ya hazina kwa
ajili ya michango, matunda ya kwanza, na zaka, ili kuzikusanya ndani yao sehemu
zinazohitajika katika sheria za makuhani na Walawi. Kila mmoja aliteuliwa kufanya
kazi mashambani karibu na miji. Kwa maana Yuda alifurahi juu ya makuhani na
Walawi waliokuwa wamesimama mbele yao. 45 Walifanya utumishi wa Mungu wao,
na huduma ya utakaso, kwa mujibu wa amri ya Daudi na ya mwanawe Sulemani, na
hivyo 46 Zamani za kale, katika siku za Daudi na Asafu, kulikuwa na wasimamizi wa
waimbaji, na kulikuwa na nyimbo za sifa na shukrani kwa Mungu. 47 Katika siku za
Zerubabeli na katika siku za Nehemia, Israeli wote walitoa sehemu za kila siku kwa
waimbaji na walinzi wa mlango. Wakaweka pembeni sehemu ya Walawi, na Walawi
waliweka sehemu ya wana wa Haruni.

# 13

1 Siku hiyo walisoma Kitabu cha Musa katika masikio ya watu. Ilionekana
imeandikwa ndani yake kwamba hakuna Mwamoni au Mmoabu anapaswa kuja
katika kusanyiko la Mungu, milele. 2 Hii ilikuwa kwa sababu hawakuja kwa watu
wa Israeli na mkate na maji, bali walikuwa wamemwajiri Balaamu kulaani Israeli.
Hata hivyo, Mungu wetu aligeuza laana kuwa baraka. 3 Mara tu waliposikia sheria,
waliwatenga Israeli toka kwa kila mgeni. 4 Sasa kabla ya hapo Eliashibu kuhani
akawekwa juu ya vyumba vya nyumba ya Mungu wetu. Alikuwa na uhusiano
na Tobia. 5 Eliashibu alimuandalia Tobia chumba kikubwa, ambako hapo awali

waliweka sadaka ya nafaka, uvumba, makala, na sehemu ya kumi ya nafaka, divai,
na mafuta, ambazo ziliwekwa kwa ajili ya Walawi, waimbaji, walinzi wa mlango,
na michango kwa makuhani. 6 Lakini wakati huu wote sikuwepo Yerusalemu. Kwa
mwaka wa thelathini na mbili wa Artashasta mfalme wa Babeli, nilikwenda kwa
mfalme. Baada ya muda nikamwomba mfalme ruhusa ya kuondoka, 7 na nikarudi
Yerusalemu. Nikafahamu mabaya ambayo Eliashibu alikuwa amefanya kwa kumpa
Tobia chumba cha kuhifadhi katika mahakama ya nyumba ya Mungu. 8 Nilikuwa na
hasira sana na nikatupa vitabu vya nyumba ya Tobia nje ya chumba cha kuhifadhi.
9 Niliamuru kwamba watakase vituo vya kuhifadhi, nami nikarudisha ndani yao
makala ya nyumba ya Mungu, sadaka ya nafaka, na uvumba. 10 Niligundua kwamba
sehemu zilizotolewa kwa ajili ya kuwapa Walawi hazikutolewa kwao, ili waweze
kuondoka haraka hekaluni, kila mmoja kwenda shambani kwake, kama waimbaji
waliofanya walivyoondoka. 11 Kwa hiyo nikawasiliana na maafisa na kusema,
'Kwa nini nyumba ya Mungu imeachwa?' Niliwakusanya pamoja na kuwaweka
kwenye nafasi zao. 12 Kisha Yuda wote wakaleta zaka ya nafaka, divai mpya, na
mafuta kwenye vituo vya kuhifadhi. 13 Nikawaweka kama watunza hazina juu
ya hazina, Shelemia kuhani, na Sadoki mwandishi, na Walawi, Pedaya. Hanani,
mwana wa Zakuri, mwana wa Matania, alikuwa na wafuasi wao, kwa sababu
walihesabiwa kuwa waaminifu. Kazi yao ilikuwa kusambaza vifaa kwa washirika
wao. 14 Nikumbuke, Ee Mungu wangu, juu ya hili, wala usiondoe matendo mema
niliyoyatenda kwa ajili ya nyumba ya Mungu wangu na huduma zake. 15 Siku hizo
nikaona watu wa Yuda waliokanyaga mvinyo siku ya Sabato, na kuleta makundi ya
nafaka, na kuwapakia punda, na divai, na zabibu, na tini, na kila aina ya mizigo
nzito, waliyoleta Yerusalemu siku ya Sabato. Nikashuhudia kuwa walikuwa wakiuza
chakula siku hiyo. 16 Watu kutoka Tiro waliokaa Yerusalemu walileta samaki na kila
aina ya bidhaa, na wakawauza siku ya Sabato kwa watu wa Yuda na katika mji!
17 Kisha nikawaambia viongozi wa Yuda, “Je! ni ubaya gani huu mnafanya, kuinajisi
siku ya Sabato? 18 Je! Baba zenu hawakufanya hivyo? Je, Mungu wetu hakuleta
mabaya haya juu yetu na juu ya mji huu? Sasa unaleta ghadhabu zaidi juu ya Israeli
kwa kudharau Sabato.” 19 Mara ilipokuwa giza kwenye milango ya Yerusalemu kabla
ya Sabato, niliamuru milango ifungwe na kwamba haifai kufunguliwa hadi baada ya
Sabato. Niliwaweka baadhi ya watumishi wangu kwenye malango ili mzigo wowote
usiweze kuletwa siku ya Sabato. 20 Wafanyabiashara na wauzaji wa kila aina ya
bidhaa walikimbia nje ya Yerusalemu mara moja au mbili. 21 Lakini niliwaonya,
“Mbona mnakaa nje ya ukuta? Ikiwa mtafanya hivyo tena, nitakuweka mikononi!”
Kutoka wakati huo hawakuja siku ya sabato. 22 Nikawaamuru Walawi kujitakasa, na
kuja kulinda milango, ili kutakasa siku ya Sabato. Nikumbuke kwa hili pia, Mungu
wangu, na kunipatia huruma kwa sababu ya uaminifu wa agano ulilonalo kwangu.
23 Katika siku hizo niliona Wayahudi waliokuwa wameoa wanawake wa Ashdodi,
Amoni na Moabu. 24 Nusu ya watoto wao walizungumza lugha ya Ashdodi, lakini
hawakuweza kuzungumza lugha ya Yuda, lakini lugha ya mmoja wa watu wengine.
25 Nami nikawasiliana nao, na mimi niliwaadhibu, na nikawapiga baadhi yao na
kuvuta nywele zao. Naliwaapisha kwa Mungu, nikisema, Msiwape wana wao binti
zenu, wala msiwachukue binti zao kwa ajili ya wana wenu, wala ninyi wenyewe. 26 Je,
Sulemani mfalme wa Israeli hakufanya dhambi kwa sababu ya wanawake hawa?
Miongoni mwa mataifa mengi hapakuwa na mfalme kama yeye, na alipendwa na
Mungu wake. Mungu akamfanya awe mfalme juu ya Israeli wote. Hata hivyo, wake
zake wa kigeni walimfanya atende dhambi. 27 Je, tunapaswa kukusikiliza na kufanya
uovu huu hata kumhalifu Mungu wetu na kuwaoa wanawake wageni? 28 Mmoja wa
wana wa Yoyada, mwana wa Eliashibu, kuhani mkuu, alikuwa mkwewe na Sanbalati

Mhoroni. Kwa hiyo nilimondoa kutoka mbele yangu. 29 Wakukumbushe, Mungu
wangu, kwa sababu wameunajisi ukuhani, na agano la ukuhani na Walawi. 30 Kwa
hiyo nimewatakasa kutoka kila kitu kigeni, na kuimarisha kazi za makuhani na
Walawi, kila mmoja kwa kazi yake mwenyewe. 31 Nilitoa sadaka za kuni wakati
uliowekwa na matunda ya kwanza. Nikumbuke, Mungu wangu, kwa mema.

# Esta

[1] Katika siku za utawala wa Ahasuero (huyu ni Ahasuero aliyetawala toka India
hadi Ethiopa, zaidi ya majimbo 127), [2] katika siku hizo Mfalme Ahasuero aliketi katika
kiti chake cha utawala katika ngome ya Shushani. [3] mwaka wa tatu wa utawala
wake aliwaandalia sherehe viongozi na watumwa wake wote. Waliohudhuria katika
sherehe hiyo walikuwa wakuu wa jeshi la Uajemi na Umedi, watu wenye vyeo, na
viongozi wa majimbo. [4] Mfalme akaweka wazi utajiri na utukufu wa ufalme wake
na heshima ya ukufu wa ukuu alio upata kwa siku nyingi, kwa siku180. [5] Siku
hizi zilipotimia, Mfalme aliaandaa karamu iliyodumu kwa siku saba. Karamu hii
ilikuwa kwa watu wote walioishi katika ikulu ya Shushani, tangu mkubwa hadi
mdogo. Behewa la bustani ya ikulu ya mfalme ndiyo karamu ilipofanyikia. [6] Behewa
la bustani lilipambwa kwa mapazia meupe ya pamba na urujuani, yalifungwa kwa
kamba za kitani safi na zambarau, yakiwa yametundikwa kwa pete za fedha na nguzo
za marimari. Kulikuwa na makochi ya dhahabu na fedha juu ya sakafu ya marimari,
mawe mekundu na meupe, na ya manjano na meusi. [7] Vinywaji viliandaliwa katika
vikombe vya dhahabu. Na kila kikombe kilikuwa ni cha kipekee na kwa sababu
ya ukarimu wa mfalme kulikuwa mvinyo mwingi. [8] Mfalme aliwambia wahudumu
watu wagawiwe vinywaji kwa kila mtu kulingana na matakwa yake. Maana tayari
mfalme alikuwa ametoa agizo kwa watumishi wa ikulu kuwafanyia wageni kulingana
na matakwa ya kila mgeni. [9] Wanawake nao walikuwa wamealikwa katika karamu
na Malkia Vashiti katika ikulu ya Mfalme Ahusuero. [10] katika siku ya saba moyo wa
mfalme ulipokuwa na furaha kwa sababu ya mvinyo, aliwaagiza Mehumani, Biztha,
Harbona, Bigtha, Abagtha, Zethari na Karkas (hawa saba ndio waliohudumu mbele
ya mfalme) [11] kumleta Malkia Vashiti akiwa katika mavazi yake ya kimalkia. Akiwa
na lengo la kuwaonyesha watu na maakida urembo wake, maana alikuwa mrembo.
[12] Pamoja na maagizo ya Mfalme, Malkia Vashiti alikataa kwenda kama alivyokuwa
amewaagiza viongozi wake. Hivyo mfalme akakasirika sana; ghadhabu yake ikawaka
ndani yake [13] Mfalme akawandea wenye hekima, waliofahamu nyakati (kwa kuwa
huu ndio uliokuwa utaratibu wa mfalme kuhusu wale waliokuwa watalaamu wa
sheria na hukumu. [14] Carshena, Shethar, Admatha, Tarshish, Meres, Marsena, na
Memucan, majimbo saba ya Uajemi na Umedi walikuwa karibu na mfalme na
walikuwa na vyeo vikubwa katika ufalme. [15] Katika kutafsiri nini kifanyike kwa
mjibu wa sheria kutoka na mgomo wa Malkia Vashiti dhidi ya agizo la mfalme
Ahusiero kwa Malkia Vashiti. [16] Mmoja wao aliyejulikana kwa jina la Memukani
alisema mbele ya Mfalme na mbele ya viongozi, Malkia Vashiti hajamkosea tu mfame
na wakuu na watu wote walio katika majimbo ya mfale Ahusiero. [17] kwa kuwa
jambo la malkia litafahamika kwa wanawake wote. watawatendea waume zao
vibaya. Watasema, 'Mfalme Ahusiero Malkia Vashiti hakumtii mme wake, Mfalme
Ahusiero alipotaka ahudhurie mbele yake.' [18] Kabla ya siku hii wanawake wa wakuu
wa Uajemi na Umedi walipata taarifa ya mgomo wa malkia Vashiti watawatendea
waume zao, viongozi wa mfalme. kutakuwa na ghasia na nyingi hasira. [19] kama ni
jambo jema kwa mfalme, ruhusu tangazo litolewe, na iwe katika sheria ya Waajemi
na Wamedi, ambao haiwezi kutanguliwa, kwamba Vashiti hatakuja tena mbele za
mfalme kama malkia. Nafasi ya Vashiti apewe mwingine ambaye ni bora zaidi ya
Vashiti. [20] Tangazo la mfalme litakapotolewa katika ufalme wote, wanawake wote
watawaheshimu waume zao, tangu mwenye cheo hadi asiye na cheo.” [21] Ushauri huu
ulikuwa mzuri kwa mfalme na wakuu wengine, mfalme akafamya kama Memkani

alivyopendekeza. [22] Akatuma barua katika majimbo yote ya mfalme, kwa kilajambo
na andiko lake, na watu kwa makabila yao. Aliamuru kwamba kila mme awe
msimamizi katika nyumba yake mwenyewe. Tangazo hili lilitolewa katika lungha
ya kila mtu katika ufalme.

# 2

[1] Baada ya mambo haya na baada ya hasira ya mfalme Ahusiero kutulia, alifikiri
kuhusu Malkia Vashiti na alichokuwa amekifanya na tangazo alilokuwa ameamuru
litolewe ya Vashiti kupoteza sifa za kuwa malkia. [2] Kisha vijana waliomtumikia
mfalme wakasema, mfalme atafutiwemabikira warembo. [3] Mfalme na achague
wasimamizi katika majimbo yote ya ufalme wake, ili wawakusanye mabikira
warembo wote harem katika ikulu ya Susa. Mabikira hawa wawe chini ya usimamizi
wa Hegai, msimamizi, ambaye ni mkuu wa wanawake, na wapewe vipodozi vyao
vyote. [4] Na binti yule atakaye mfurahisha mfalme ndiye atakaye kuwa Malkia badala
ya Vashiti." Mfalme alupenda ushauri na akafanya kama alivoshauriwa, [5] Katika
mji wa Shushani alikuwepo Myahudi aliyeitwa Modekai mwana wa Jaira mwana wa
Shimei mwana wa Kishi, aliye kuwa wa kabila la Benjamini. [6] Yeye ni miongoni mwa
Wayahudi waliochukuliwa pamoja na Yekonia, mfalme wa Yuda kutoka Yerusalemu
na kupelekwa uhamishoni na mfalme Nebukadreza. [7] Modekai alikuwa akimlea,
Hadasa, yaani Esta, binti wa mjomba wake kwa sababu hakuwa na wazaai wake
wote wawili. Modekai alimchukuwa kama binti yake. Esta alikuwa na umbo zuri na
uso wa kupendeza. [8] Wasichana wengi waliletwa ikulu Shushani, baada ya tangazo
na amri ya mfalme kutolewa. Waliwekwa chini ya usimamizi wa Hegai. Esta naye
alikuwa ni miongoni mwa wasichana walioletwa na kuwekwa chini ya usimamizi wa
Hegai, mwangalizi wa wanawake. [9] Esta alimfurahisha, na akapata kibali mbele ya
Hegai. Akampa vipodozi na sehemu ya chakula. Akampa wahudumu wa kike saba
kutoka katika ikulu ya mfalme, na akampeleka na wahudumu wa kike katika sehemu
bora katika nyumba ya wanawake. [10] Esta hakuwa amemweleza mtu yeyote kuhusu
jamaa zake kwa sababu Modekai alikuwa amemzuia. [11] kila siku Modekai alienda
na kurudi mbele nje ya ua wa nyumba ya wanawake, ili kwamba asikie kuhusu
mambo ya Esta na atakachofanyiwa. [12] Zamu ilipofika ya kila msichana kwenda kwa
mfalme Ahusero kwa kufuata maelekezo kwa wanawake, kila msichana alitakiwa
kumaliza miezi kumi na miwili ya urembo, miezi sita ya mafuta ya manemane na
miezi sita ya vipodozi. [13] wakati msichana alipoenda kwa mfalme, alipewa chochote
alichotamani kutoka katika nyumba ya wanawake ili aende nacho katika nyuma ya
mfalme. [14] Msichana alipaswa kwenda wakati wa usiku na kurudi katika nyumba ya
wanawake, na kwa msimamizi Shaashigazi, msimamizi wa mfalme, ambaye alikuwa
mwenye kuwalinda masulia. Msichana hakuruhusiwa kwenda tena kwa mfalme
isipokuwa amemfurahiha mfalme na mfalme akaamuru arudi tena. [15] Zamu ya
Esta ilipotimia( mwana wa Abihaili, mjomba wa Modekai alikuw amemchukua kama
kama binti yake) kwenda mbele ya mfalme, hakutaka kitu chochote isipokuwa vile
ambavyo Hegai, msimamizi wa wanawake alimtaka avichukue. [16] Esta akapata kibali
mbele ya kila aliyemwona. Esta akapelekwa kwa Mfalme Ahusiero katika makazi
ya kifalme mwezi wa kumi, ambao ni mwezi wa Tabeti, katika mwaka wa saba
wa utawala wake. [17] Mfalme alimpenda Esta zaidi kuliko wanawake wengine, na
alipata kibali kuliko na wema mbele zake zaidi kuliko mabikira wengine na hivyo
mfalme akamvika taji ya kimalkia badala ya Vashiti. [18] mfalme akawafanyia karamu
kubwa wasimamizi na wahudumu wake wote, karamu ya Esta na akawapa unafuu
wa kodi katika majimbo. Pia akawapa zawadi kwa ukarimu. [19] Modekai alikuwa
ameketi katika lango la mfalme wakati mabikira walipokuwa wamekusanyika kwa

mara ya pili. [20] Esta alifuata ushauri Modekai ya kutomwambia mtu yeyote kuhusu
jamaa zake. aliendelea kufuata ushauri wa Modekai kama alivyofanya alipokuwa
mdogo. [21] katika siku hizo ambazo Modekai alikuwa ameketi getini kwa mfalme,
Bighani na Tereshi, wasimamizi wa mfalme walio linda lando, walikasirika na
wakatafuta kumuua mfalme Ahusiero. [22] Jambo lilipowekwa wazi kwa Modekai,
alimtaarifu Malkia Esta na Esta akamweleza kile achoelezwa na Modekai. [23] Habari
hii ilipepelelezwa na kuonekana kuwa kweli na wanaume wawili walinyongwa juu
ya mti. Na habari hii ikaandikwa katika kitabu cha taarifa mbele ya mfalme.

# 3

[1] Baada ya mambo haya, Mfalme Ahusiero alimpandisha cheo Hamani mwana
wa Hammedatha mwagagi, na akaweka kiti chake cha ukuu juu ya wakuu wote
waliokuwa pamoja naye. [2] Na watumishi wote wa mfalme waliokuwa katika lango la
mfalme walipaswa kupiga magoti na kusujudia Hamani, kama mfalme alivyoagiza.
Lakini Modekai hakupiga magoti wala kusujudu mbele ya Hamani. [3] Kisha watumishi
wa mfalme waliokuwa langoni mwa mfalme walimwambia Modekai, kwa nini hautii
amri ya mfalme? [4] Walisema naye siku kwa siku, lakini alikataa kufuata matakwa
yao. Hivyo wakaongea na Hamani kuona kama swala la Modekai lingebaki hivyo
alikuwa amewataarifu kuwa Modekai alikuwa Muyahudi. [5] Hamani alipoona kuwa
Modekai hapigi magoti wala kumsujudia, alipatwa na hasira. [6] Alikuwa na wazo
la kumuua Modekai, watumishi wa mfalme walikuwa wamemueleza kuwa Modekai
na jamaa zake walikuwa Wayahudi. Hamani akaazimu kuwaangamiza Wayahudi
wote, watu wa Modekai, ambao walikuwa katika ufalme wa Ahusiero. [7] Katika
mwezi wa kwanza, (ambao ni mwezi wa Nisani) ndani ya mwaka wa kumi na
mbili wa Mfalme Ahusiero, walipiga kura mbele ya Hamani kura kila siku na
mwezi, kuchagua siku na mwezi hadi walipochagua mwezi wa kumi na mbili,
(mwezi wa Adari. [8] Kisha Hamani akamwambia mfalme Ahusiro, “kuna watu fulani
katika majimbo yote ya ufalme wako wasiofuata sheria zako. Na kwa tabia yao ya
kutofuata sheria zako hawapasi kuendelea kuwa hai. [9] Kama ikimpendeza mfalme,
toa amri watu hawa wote wakatiliwe mbali, nami nitapima talanta elfu kumi za
fedha katika mikono ya wale ambao ni wasimamizi wa maswala ya mfalme, ili
kwamba waweke katika hazina ya mfalme.” [10] Ndipo mfamle akavua pete yake ya
muhuri na kumpa Hamani, adui wa Wayahudi. [11] Mfalme akamwambia Hamani,
“Nitahakikisha kwamba fedha inarudi kwako na kwa watu wako. Ili muitumie kama
mpendavyo.” [12] Kisha waandishi wa mfalme walikusanyika katika siku ya kumi na
tatu ya mwezi wa kwanza, na mbiu iliyokuwa na matakwa ya Hamani yalikuwa
yameandikwa na kupelekwa kwa wasimamizi wa majimbo, na wale wote waliokuwa
juu ya wasimamizi wa majimbo yote, na wasimamizi wa watu, na kwa kila jimbo
kwa andiko lao, na kila watu na lugha yao. Mbiu hii ilikuwa imeandikwa kwa jina
la mfalme Ahusiero na kupigwa muhuri wa pete yake. [13] Barua hizi za kutaka
kuwakatilia mbali Wayahudi wote zilizambazwa katika majimbo yote ya Mfalme
Ahusiero, kuangamiza, kuua na kuwaharibu Wayahudi wote, tangu mdogo hadi
mkubwa, watoto na wanawake, ndani ya siku moja katika siku ya kumi na tatu ya
mwezi wa kumi na mbili (ambao ni mwezi wa Adari) na kuteka mali zo. [14] Nakala
ya ilifanywa kuwa sheria na kupelekwa kila jimbo. Taarifa juu ya maangamizi
ya Wayahudi ilienea katika kila jimbo kwamba watu wote wajiandae katika siku
hiyo. [15] Wasambazajia walisambaza agizo la mfalme. Tangazo hili pioa lilitolewa
na kusambazwa katika mji wa Shushani. Mfalme alikuwa na Hamani walikaa na
kunywa, lakini mji wa Shushani, lakini mjiwa Shushani ulikuwa katika uangamivu.

# 4

1 Modeka aliposikia kilichokuwa kimepangwa dhidi yao, alirarua mavazi yake na
kuvaa maguni na majivu. Akaenda katikati mwa mji na kulia kwa sauti na uchungu
mwingi. 2 Akaenda hadi langoni mwa mfalme; kwa sababu hakuna aliye ruhusiwa
kuingia akiwa amevaa magunia. 3 Amri hii ilipofika katika kila jimbo, kulikuwa na
kilio kikubwa kwa Wayahudi, na kufunga, kulia na maombolezo. Wengi wao walilala
katika magunia na majivu. 4 Malkia Esta alipopata habari kutoka kwa wahudumu
wake, alipatwa na majonzi. Akatuma watu wampelekee nguo Modekai ili avue
magunia na kuvaa nguo nzuri, lakini Modekai hakukubali. 5 kisha Esta akamwita
Hathaki, mmoja wa wasimamizi wa mfalme, ambaye alikuwa amepewa wajibu wa
kumuhudumia. Akamwagiza kwenda kwa Modekai ili afahamu kwa nini Modekai
ameamua kufanya hivyo. 6 Hivyo Hathaki akaenda kwa Modekai katika mji mbele
ya lango la mfalme. 7 Modekai akamweleza Hathaki mambo yote kuhusu maangamizi
ya Wayahudi yaliyo pangwa na kiasi cha fedha ambacho Hamani ameahidi kuwapa
wahazini wa mfalme, ili kuwaua Wayahudi. 8 Na kisha akampa nakala ya mbiu
ambayo ilitolewa Shushani kwa uangamivu wa Wayahudi. Alifanya hiivyo ili
kwamba Hathaki amwambie Esta achukue jukumu la kwenda na kumuomba mfalme
na kumsihi kwa niaba ya Wayahudi. 9 Hivyo, Hathaki akaenda na kumweleza Esta
kile alicho ambiwa na Modekai. 10 Esta akaongea na Hathaki na akamwambia arudi
kwa Modekai. 11 Esta akamwambia Hathaki, "Watumishi wote wa mfalme na watu
wote katika majimbo yote wanafahamu kuwa mtu yeyote aingiae kwa mfalme bila
kibali anapaswa kufa isipokuwa yule ambaye mfalme atamunyoshea fimbo yake ya
dhahabu. Ni siku thelathini sasa sijaenda mbele ya mfalme. 12 Hathaki akamwambia
Modekai maneno aliyoambiwa na Esta. 13 Modekai akarudisha ujumbe: "usifikiri
kwamba wewe utasalimika kuliko Wayahudi wote. 14 Kama ukikaa kimya kwa wakati
huu, Mungu ataleta wokovu kwa njia nyingine, lakini wewe na nyumba ya baba yako
mtaangamia. Ni nani ajuaye umekuja katika nafasi hii kwa wakati muafaka kama
huu. 15 Kisha Esta akatuma ujumbe kwa Modekai, 16 "Nenda, uwakusanyea Wayahudi
wote wanaoishi katika mji wa Shushani, na wafunge kwa ajili yangu. Wasile wala
kunywa kwa muda wa siku tatu. Mimi na watumishi watumishi wangu wa kike
tutafunga kwa siku hizo. Na kisha nitaenda mbele ya mfalme kinyume cha sheria.
Na kama nitakufa na nife. 17 Modekai akaenda na akafanya yote ambayo Esta aliyo
mwagiza kufanya.

# 5

1 Baada ya siku tatu, Esta akajivika mavazi yake ya kimalkia na akasimama sehemu
ya ndani ya ua wa ikulu ya mfalme, mbele ya nyumba ya mfalme. mfalme alikuwa
ameketi katika kiti chake cha enzi na akitazama mlango wa kuingilia. 2 Mfalme
alipomwona malkia Esta alipata kibali kwa mfalme. Alimpa fimbo ya dhahabu
mikononi mwa Esta. Hivyo Esta akamsogelea mfalme na kuishika fimbo ya utawala.
3 Kisha mfalme akamwambia Malkia Esta, "Unahitaji upewe nini? Ombi lako ni lipi?
Hata nusu ya ufalme wangu utapewa." 4 Malkia Esta akamwambia mfalme, kama
nimepata kibali machoni pako, naomba wewe na Hamani muhudhurie leo katika
karamu niliyoiandaa kwa ajili yake." 5 Mfalme akasema, "Mleteni haraka Hamani
sawa sawa na matakwa ya Malkia Esta." Mfalme pamoja na Hamani wakahuduria
katika karamu aliyoandaa malkia Esta. 6 Mvinyo ulipohudumiwa katika karamu,
mfalme akamuuliza Malkia Esta hitaji lako ni nini? Na ombi lako ni lipi? Utapewa
hata nusu ya ufalme." 7 Esta akajibu mfalme, "Hitaji na ombi langu ni hili, 8 kama
ikikupendeza mfalme, kwa kunipa haja yangu na kuheshimu ombi langu, wewe
na Hamani muhudhurie tena katika karamu nitakayoiandaa kesho na hapo ndipo

nitakapo kuambia haja yangu. 9 Hamani akaenda nyumbani kwakwe huku akiwa
amejawa na furaha moyoni mwake. Lakini alipomwona Modekai katika lango la
mfalme, modekai hasimami wala kutetemeka mbele zake, alijawa na ghadhabu kwa
ajili ya Modekai. 10 Lakini akajizuia na akaenda nyumbani kwake. Akawaarika
marafiki zake wakakusanyika pamoja na Zereshi, mkewe. 11 Hamani akawaeleza
juu ya utukufu wa mali na idadi ya watoto aliokuwa nao, na vile alivyo juu kuliko
wasimamizi na watumishi wote wa mfalme. 12 Hamani akawambia, “Hata jana
Malkia Esta aliandaa karamu kwa ajili ya mfalme na ni mimi tu na mfalme tulio
hudhuria katika karamu aliyoiandaa Malkia Esta. Na hata kesho tuna mwaliko
mwingine pamoja na mfalme. 13 Lakini haya yote sio kitu kama Modekai ataendelea
kukaa katika lango la mfalme. 14 Kisha Zereshi, mkewe Hamani akamwambia
Mmewe na rafiki zake wote, “Andaeni mti wenye urefu wa futi hamsini. Na wakati
wa ahsubuhi ongea na mfalme ili Modekai atundikwe katika mti huo. Kisha nenda
kwa furaha na mfalme katika karamu aliyoiandaa Malkia.

# 6

1 Usiku ule mfalme hakupata usingizi. Akaagiza vitabu vya kumbukumbu vya
matukio ya ufalme wake viletwe na visomwe mbele zake. Vitabu visomwa kwa sauti
mbele ya mfalme. 2 Ikakutwa kuwa Modekai alikuwa ametoa taarifa kuhusu Bighana
na Tereshi, walinzi walio linda lango, waliokuwa wamepanga kumuangamiza Mfalme
Ahusiero. 3 Kisha mfalme akauliza, Modekai alifanyiwa nini cha heshima kwa kwa
taarifa aliyoitoa? Ndipo watumishi wa mfalme wakamwambia, “Hakufanyiwa kitu
chochote.” 4 Kisha mfalme akauliza, “Ni nani aliye ndani ya ua.” Na Hamani
alikuwa ameingia katika ua wa mfalme ili amwombe mfalme atoe kibali ili Modekai
atundikwe kwenye mti aliouandaa. 5 Watumishi wakamjibu, “Hamani amesimama
katika ua ya mfalme.” Mfalme akasema, “Mwambieni aingie ndani.” 6 Mara tu
Hamani alipoingia, mfalme akamuuliza, afanyiewe nini mtu yule ambaye mfalme
anampenda na kumheshimu?” Hamani akafikiri moyoni mwake, “Ni nani ambaye
mfalme ampenda na kumuheshimu zaidi yangu? 7 Hamani amjibu mfame, Kwa
mtu yule ambaye mfalme ampenda na kumuheshimu, 8 avikwe nguo za kifalme,
mavazi ambayo mfalme amekwisha yavaa na farasi ambaye ametumiwa na mfalme
na ambaye ana taji ya kifalme kichwani mwake. 9 Nguo hizo na farasi apewe
msimamizi bora kuliko wote. Na wamvike yule ambaye mfalme ampenda na
kumuheshimu, na wampandishe juu ya farasi na kumpitisha katika mitaa yote
ya mji. Na watangaze mbele yake, “Hivi ndivyo alivyofanyiwa mtu yule ambaye
mfalme ampenda na kumuheshimu!” 10 Kisha mfalme akamwambia, Hamani “fanya
hima, mvike Modekai nguo na umpandishe kwenye farasi, na lisipungue hata jambo
moja katika hayo uliyo yasema.” 11 Kisha Hamani akachukua mavazi na farasi.
Akamvika Modekai na akampandisha kwenye farasi na kumpitisha katika mitaa
yote ya mji. Akatangaza mbele zake, “Hii imefanyika kwa mtu ambaye mfalme
anampenda na kumuheshimu!” 12 Baada ya hayo Modekai alirudi kwenye lango
la mfalme. Huku Hamani akarudi kwa haraka nyumbani kwake, huku akiomboleza,
na akiwa ameinamisha kichwa chake. 13 Akawaeleza rafiki zake pamoja na Zereshi
mkewe. Kisha rafiki zake wenye hekima pamoja na Zereshi mkewe. Kama Modekai,
ambaye umeanza kuanguka mbele zake ni wa uzao wa Wayahudi, hautamshinda,
bali utandelea kuanguka mbele zake.” 14 Walipokuwa wakiendelea na maongezi,
wasimamizi wa mfalme wakamjia Hamani ili aende kwenye karamu aliyoiandaa
Esta.

# 7

1 Kwa hiyo mfalme na Hamani wakaenda kausherekea na malkia Esta. 2 Katika
siku ya pili, baada ya kuletwa mvinyo, mfalme akamwambia Esta, “Ni nini haja
ya moyo wako? Na nini ombi lako? Hata nusu ya ufalme wangu utapewa.”
3 Kisha Malkia amwambia mfalme, kama nimepata kibali machoni pako, na kama
ikikupendeza, nipewe maisha yangu, na hili ndio haja ya moyo wangu, na hili pia
ni ombi kwa watu wangu pia. 4 Kwa kuwa mimi na watu wangu tumeuzwa, ili
tuharibiwe, tuuwawe, na tungamizwe. Kama tungeuzwa utumwani, kama wanaume
na wanawake, ningenyamaza kimya, na nisingeweza kumsumbua mfame.” 5 Kisha
Mfalme Ahusiero akamwambia malkia Esta, “Ni nani huyo? Ni nani aliyekusudia
moyoni mwake kutenda jambo hili? 6 Esta akasema, “Ni huyu mwovu Hamani, adui!”
Hamani akashikwa na Hofu mbele za mfalme na malkia. 7 Na kwa ghadhabu mfalme
akatoka karamuni katika sehemu ya mvinyo na akaenda katika bustani ya ikulu,
Lakini Hamani alibaki akimsihi Malkia Esta ili aokoe maisha yake. Kwa sababu
aliona mfalme amemkusudia ubaya. 8 Mfalme akarudi kutoka katika bustani ya
ikulu, na kuingia katika chumba ambamo kulikuwamo mvinyo. Hamani alikuwa
ameanguka chini ya kochi alilokuwa ameketi Esta. Mfalme akakasirika na kusema,
“atamdharirisha malkia mbele zangu katika nyumba yangu?” Mara tu maneno haya
yalipotoka kinywani mwa mfalme, watumizhi wakafunika uso wa Hamani. 9 Kisha
Habona, mmoja wa watumishi aliye mtumikia mfalme akamwambia mfalme, “Mti
wenye urefu wa futi hamsini uko nyumbani kwa Hamani. Ulikuwa umeandaliwa kwa
ajili ya Modekai, aliye toa taarifa kuhusu mpango wa kuangamizwa kwako.” Mfalme
akesema,”Mtundikeni Hamani juu yake.” 10 Kwa hiyo wakamtundika Hamani
kwenye mti aliuandaa kwa ajili ya Modekai. Na hasira ya mfalme ikatulia.

# 8

1 Siku hiyo Mfalme Ahusiero akampa Malkia Esta mali yote ya Hamani, adui wa
Wayahudi. Na kisha akampandisha cheo Modekai ili atumike mbele zake, kwa
sababu Malkia Esta alikuwa amemueleza Mfalme uhusiano wake na Modekai. 2 Kisha
Mfalme akampa pete yake aliyokuwa amempa Hamani. Malkia Esta akampandisha
Modekai ili awe mkuu katika shamba la Hamani. 3 Kisha Esta akaongea tena na
mfalme. Akaanguka chini na kulia mbele za mfalme akimsihi Mfalme abatilishe
njama ya kuwaua Wayahudi wote iliyokuwa imetangazwa na Hamani Muagagi
4 kisha mfalme akamnyoshea Esta fimbo yake ya dhahabu, akainuka na kusimama
mbele ya mfalme. 5 Esta akasema, “Kama ikikupendeza na kama nimepata kibali
mbele zako, agiza mbiu ipigwe ili kubatilisha barua zilizoandikwa na Hamani mwana
wa Hammedatha muagagi, barua alizoziandika ili kuwa angamiza Wayahudi wote
walikuwa katika majimbo yote ya mfalme. 6 Ninawezaje kuona ubaya ukiwapa watu
wangu? Ninawezaje kutazama uharibifu wa jamaa zangu?” 7 Mfalme Ahusiero
akamwambia Esta na Modekai, Muyahudi, tazama nimempa Esta nyumba yote ya
Hamani na wamemtundika Hamani katika mti kwa sababu alikuwa amekusudia
kuwaangamiza Wayahudi wote. 8 Hivyo andika mbiu nyingine kwa ajili ya Wayahudi
kwa jina la mfalme na uipige muhuri kwa pete ya mfalme. Kwa sababu mbiu
imekwisha andikwa kwa jina la mfalme na kugongwa muhuri kwa pete ya mfamle
na haiwezi kubatilishwa.” 9 Kisha waandishi wa mfalme wakakusanyika kwa wakati
huo huo katika mwezi wa tatu, ambao ni mwezi wa Sivani, siku ya ishirini ya
mwezi wa tatu. Mbiu iliandikwa yote ambayo Modekai aliyaamuru kwa Wayahudi
watendewe na wenyeji wa kila jimbo. Mbiu iliandikwa kwa maakida magavana
na wakuu wa majimbo yote yaliyokuwa toka India hadi Ethiopia, majimbo 127
kila jimbo iliandikwa kuwa maandishi yake, na kila watu kwa lugha yao, na kwa
Wayahudi kwa maandishi na lugha yao. 10 Modekai akaandika kwa jina la Mfalme

Ahusiero na akazipiga muhuri kwa pete ya mfalme. Akapeleka nyaraka kwa
matarishi, akawapandisha kwenye farasi waendao kwa haraka waliotumika kwa
huduma ya mfalme, waliozaliwa kwa mfalme. 11 Mfalme akawapa Wayahudi wote
katika majimbo ya utawala wake kibali cha kukusanyika na kujilinda na ruhusa ya
kuangamiza, kuua na kuharibu mtu yeyote aliyekuwa na kusudi la kuwaua Wayahudi
wote na kupora mali zao. 12 Jambo hili lilipaswa litekelezwe katika majimbo yote ya
Mfalme Ahusiero, siku ya ya kumi na tatu ya mwezi wa kumi na mbili, ambao ni
mwezi wa Adari. 13 Nakala ya mbiu ilipaswa kutolewa kama sheria na kutangazwa
kwa watu wote. Wayahudi walikuwa tayari kwa siku hiyo kulipa kisasi kwa adui
zao. 14 Hivyo matarishi wakaendesha farasi waliokuwa wakitumiwa katika huduma
za kifalme. Walienda kwa haraka sana. Mbiu hii pia ilikuwa imetolewa katika mji wa
Shushani pia. 15 Kisha Mosekai akaondoka mbele za mfalme akiwa amevaa mavazi
ya kifalme, nguo buluu na nyeupe na taji kubwa ya dhahabu na joho la zambarau.
Mji wa Shushani ukafurahia. 16 Wayahudi walikuwa na nuru, na furaha na heshima.
Mji wowote ambao mbiu hii ilipigwa, Wayahudi walifurahia na walifanya karamu na
pumziko. 17 Watu wengi wakatamani kuwa Wayahudi sababu ya hofu ya Wayahudi
iliyokuwa juu yao.

# 9

1 Sasa katika mwezi wa kumi na mbili, siku ya kumi na tatu ambayo ni siku ya
Adari, siku ambayo adui wa Wayahudi walitarajia kutekeleza sheria ya mfalme na
kupata nguvu dhidi ya Wayahudi. Badala yake Wayahudi wakapata nguvu dhidi
ya adui zao. 2 Wayahudi wote wakakusanyika katika miji yao katika majimbo
yote ya Mfalme Ahusiero, kutia mikono juu ya wale waliokusudia ubaya. Hakuna
aliye kuwa tayari kusimama zao kwa sababu hofu yao ilikuwa imewaangukia
watu wote. 3 Wakuu wote wa majimbo, maakida na magavana, na watawala wa
mfalme, waliwasaidia Wayahudi kwa kuwa hofu ya Modekai ilikuwa imewaangukia.
4 Kwa kuwa Modekai alikuwa mkuu katika nyumba ya mfalme, na umaarufu wake
ukasambaa katika majimbo yote, kwa kuwa Modekai alikuwa akifanyika mkuu.
5 Wayahudi wakawavamia maadi zao kwa upanga, wakiwatenda vibaya kama
walivyokuwa wamekusudiwa mabaya dhidi yao Wakawatenda kama walivyo ona
vyema machoni pao. 6 Katika ngome ya mji wa Shushani pekee jumla ya maadui
waliouawa na na kuharibiwa na Wayahudi ni wanaume mia tano. 7 Miongoni
mwa waliouawa ni pamoja na Parishandatha, Dalphoni, Aspatha, 8 Poratha, Adalia,
Aridatha, 9 Parimashita, Arisai, Aridai, Vaizatha, 10 na wana kumi wa Hamani,
mwana wa Hammedatha, adui wa Wayahudi. Lakini hawakuchua mateka yoyote.
11 Idadi ya wale waliouawa siku hiyo katika mji wa Shushani, ilifikishwa kwa
Mfalme Ahusiero. 12 Mfalme akamwambia malkia Esta. Mfalme akamwambia
Malkia Esta, “Wayahudi wameua wanaume mia tano katika mji wa Shushani,
wakiwemo wana kumi wa Hamani adui wa Wayahudi. Je wamefanya nini katika
majimbo mengine? Na sasa haja yako ni nini? Utapewa. Ombi lako ni nini?”
13 Esta akamjibu, “Mfalme kama ikikupendeza, ruhusu Wayuadi walio katika mji
wa Shushani wapige mbiu hii na kesho, na miili ya watoto wa Hamani itundikwe
juu ya miti.” 14 Mfalme akaamuru ombi la Esta litekelezwe. Mbiu ilipigwa katika mji
wa Shushani, na wana kumi wa Hamani wakatundikwa juu ya miti. 15 Wayahudi
katika mji wa Shushani walisanyika pamoja siku ya kumi na nne ya mwezi wa
Adari, na kuwaua maadui zao mia tatu katika mji wa Shushani, lakini hawakugusa
nyara zao. 16 Na Wayahudi katika majimbo mengine wakakusanyika ili kujilinda
na wakapata faraja kutoka kwa maadui na wakawaua maadui zao elfu sabini na
tano, lakini hawakugusa mikono yao kwa vitu vya thamani wale waliouwawa.

17 Katika siku ya kumi na tatu ya mwezi wa Adari, Wayahudi wakapumzika katika
siku ya kumi na nne, wakapumzika siku hiyo ya karamu na furaha. 18 Lakini
Wayahudi walioishi katika mji wa Shushani wakaja pamoja siku ya kumi na tatu
na ya kumi na nne. Na siku ya kumi na tano wakapumzika na wafanya karamu na
kufurahia. 19 Hii ndiyo sababu Wayahudi wa vijijini, wanaishi maeneo ya vijijini,
huadhimisha siku ya kumi na nne ya mwezi wa Adari kama siku ya furaha na
karamu na siku ambayo hutumiana zawadi kwa kila mmoja. 20 Modekai akaweka
mambo haya na akatuma nyaraka kwa Wayahudi wote waliokuwa katika utawala
wa Mfalme Ahusiero, 21 akiwataka kuazimisha siku ya kumi na nne na kumi na
tano ya mwezi wa Adari kila mwaka. 22 Hizi zilikuwa ndizo siku ambazo Wahudi
walipata faraja kutoka kwa maadui zao na wakati huu ndio wakati ambao huzuni
ya Wayahudi iligeuzwa kuwa furaha, na kutoka kwa maombolezo hadi kwenye
pumziko. Walipaswa kuzifanya siku za karamu na furaha, na kutumiana zawadi
ya chakula, na zawadi kwa masikini. 23 Wayahudi wakaendelea na maadhimisho
wakifanya kile ambacho Modekai alikuwa amewaandikia. 24 Na wakati huo
Modekai mwana wa Hammedatha mwagagi, adui wa Wayahudi aliyekuwa amepanga
njama ya kuwaangamiza Wayahudi, na kwa kupiga Puri (yaani akapiga kura) ili
kuwaangamiza kabisa. 25 Lakini Mfalme Ahusiero alipopata taarifa ya mpango
mbaya huu alioupanga Modekai dhidi ya Wayahudi, aliagiza kwa nyaraka afanyiwe
Modekai mwenyewe, na kwamba yeye na wana wake wanyongwe juu ya miti.
26 Hivyo Wayahudi wakaziita siku hizi Purimu, kutokana na jina Puri. Kwa sababu
ya mambo yote yaliyo kuwa yameandika katika barua, na mambo yote ambayo
walikuwa wameyaona kwa macho yao, na yale yalikuwa yamewapata, 27 Wayahudi
wakapokea jukumu na desturi mpya. Desturi hii iwe kwa ajili yao, watoto wao, na kila
ambaye aliyeungana nao. Na itakuwa kwamba maadhimisho haya watayafanya kwa
kila mwaka. Wataadhimisha kwa namna fulani na nyakati hizo hizo kila mwaka.
28 Siku hizi zilipaswa kuadhimishwa katika kila kizazi, kila familia, kila jimbo na
kwa kila mji. Wayahudi hawa na watoto wao hawakuacha kuadhimisha siku hizi
za Purimu, ili kwamba wasizisahau. 29 Malkia Esta na Modekai wakaandika kwa
mamlaka yote na kuthibitisha barua hii ya pili kuhusu Purimu. 30 Barua zilipelekwa
katika majimbo 127 ya mfalme Ahusiero, zikiwatakia Wayahudi wote amani na
kweli. 31 Na kuthibitisha siku za Purimu sawa sawa na maelekezo ya Modekai na
Esta yaliyowataka Wayahudi waadhimishe. Wayahudi wakatii maagizo kwa ajili
yao na uzao wao, kama walivyotii siku za kufunga na kuomboleza. 32 Agizo la Esta
likahakikisha sheria hizi kuhusu Purimu, na ikaandikwa katika kitabu.

# 10

1 Kisha Mfalme Ahusiero akaweka kodi juu ya nchi na maeneo ya bahari.
2 Mafanikio yote na nguvu na ukuu wake, pamoja na wa Modekai ambao mfalme
alimwinua, yameandikwa katika Kitabu cha Kumbukumbu ya wafalme wa Wamedi
na Waajemi. 3 Modekai Muyahudi alikuwa wa pili kutoka kwa Mfalme Ahusiero.
Alikuwa mkuu na maarufu miongoni mwa ndugu zake Wayahudi, kwa sababu
alitetea mahitaji ya watu wake na haki za watu na akatetea amani kwa watu wote.

# Ayubu

1 Kulikuwa na mtu katika nchi ya Usi jina lake Ayubu; na Ayubu alikuwa mwenye
haki na mkamilifu, mmoja aliyemcha Mungu na kuepukana na 2 uovu. Wakazaliwa
kwake watoto saba wa kiume na mabinti watatu. 3 Alimiliki kondoo elfu saba,
ngamia elfu tatu, jozi mia moja za maksai, na punda mia tano na idadi kubwa
ya watumishi. Mtu huyu alikuwa mtu mkuu wa watu wote wa mashariki. 4 Kwa
siku yake kila mtoto wa kiume, hufanya karamu katika nyumba yake. Wakatuma
na kuwaita dada zao watatu waje kula na kunywa pamoja nao. 5 Baada ya siku
za karamu zilipokuwa zimetimia, Ayubu hutuma kwao na kuwatakasa. Aliamka
asubuhi na mapema na kutoa sadaka za kuteketezwa kwa kila mtoto wake, kwa
kusema, “Yawezekana kwamba wanangu wamefanya dhambi na kumkufuru Mungu
mioyoni mwao.” Siku zote Ayubu alifanya hivi. 6 Kisha ilikuwa siku ambayo watoto
wa Mungu walikwenda kujihudhurisha mbele za BWANA. Shetani pia akaenda
pamoja nao. 7 BWANA akamuuliza Shetani, “Umetoka wapi wewe?” Kisha Shetani
akamjibu BWANA na kusema, “Natoka kuzunguka zunguka duniani, kutembea huku
na huko humo.” 8 BWANA akamuuliza Shetani, “Je umemwangalia mtumishi wangu
Ayubu? Kwa kuwa hakuna mmoja aliye kama yeye duniani, mtu mwenye haki
na mkamilifu, mmoja aliyemcha Mungu na kuepukana na uovu.” 9 Kisha Shetani
akamjibu BWANA na kusema, “Je Ayubu amcha Mungu bila sababu? 10 Wewe
hukumwekea kinga pande zote, kuzunguka nyumba yake, na kuzunguka vitu vyote
alivyo navyo kutoka kila upande? Wewe umebariki kazi za mikono yake, na mifugo
yake imeongezeka katika nchi. 11 Lakini sasa nyosha mkono wako na uguse yote hayo
aliyonayo, na uone kama hatakufuru mbele ya uso wako.” 12 BWANA akamwambia
Shetani, “Tazama, hayo yote aliyonayo yamo mkononi mwako. Isipokuwa juu yake
yeye mwenyewe usinyoshe mkono wako.” Kisha Shetani akatoka mbele za BWANA.
13 Ilitokea siku moja, wana wake wa kiume na binti zake walipokuwa wakila na
kunywa mvinyo nyumbani mwa ndugu yao mkubwa. 14 Mjumbe akamfikia Ayubu
na kusema, “Hao maksai walikuwa wakilima na punda walikuwa wakichunga karibu
nao. 15 Waseba wakawaangukia na kutoweka nao. Kwa wale watumishi, wamewaua
kwa makali ya upanga. Mimi pekee nimeokoka kukuletea habari.” 16 Wakati
alipokuwa akiendelea kusema, akatokea mwingine pia na kusema, “Moto wa Mungu
umeanguka toka mbinguni na kuwateketeza kondoo na watumishi. Mimi pekee
nimeokoka kukuletea habari.” 17 Wakati alipokuwa akiendelea kusema, akatokea
mwingine pia na kusema, “Wakaldayo walifanya vikundi vitatu, wakawashambulia
ngamia, na kuondoka nao. Kwa wale watumishi, wamewaua kwa makali ya upanga.
Mimi pekee nimeokoka kukuletea habari.” 18 Wakati alipokuwa akiendelea kusema,
akatokea mwingine pia na kusema, “Wana wako wa kiume na binti zako walikuwa
wakila na kunywa mvinyo nyumbani mwa ndugu yao mkubwa. 19 Upepo wenye
nguvu ulitokea jangwani na ukapiga pembe nne za nyumba. Ikawaangukia vijana
hao, na wakafa wote. Mimi pekee nimeokoka kukuletea habari. 20 Kisha Ayubu
akainuka, akalirarua joho lake, akanyoa kichwa chake, akaanguka chini kifudifudi na
kumwabudu Mungu. 21 Akasema, “Mimi nilitoka tumboni mwa mama yangu ni uchi,
nami nitakuwa uchi wakati nitakaporudi huko. BWANA alitoa, na BWANA ametwaa.
Jina la BWANA libarikiwe.” 22 Katika mambo hayo yote, Ayubu hakutenda dhambi,
wala hakumwazia Mungu kwa uovu.

# 2

1 Kisha kulikuwa na siku wana wa Mungu walipokwenda kujihudhurisha mbele za
BWANA. Shetani pia alikwenda kati yao kujihudhulisha mbele za BWANA. 2 BWANA
akamuuliza Shetani, "umetoka wapi wewe?" Kisha Shetani akamjibu BWANA na
kusema, "Natoka kuzunguka zunguka duniani, kutembea huku na huko humo."
3 BWANA akamuuliza Shetani, "Je umemwangalia mtumishi wangu Ayubu? Kwa
kuwa hapana mmoja aliye kama yeye duniani, mtu mwenye haki na mkamilifu,
mmoja aliye mcha Mungu na kuepukana na uovu. Hata sasa anashikamana na
utimilifu wake, japokuwa ulinichochea juu yake, nimwangamize pasipo sababu."
4 Shetani akamjibu BWANA na kusema, "Ngozi kwa ngozi, kweli; mtu atatoa vyote
alivyo navyo kwaajili ya uhai wake. 5 Lakini nyosha mkono wako sasa na uguse
mifupa yake na nyama yake, na uone kama hatakufuru mbele ya uso wako."
6 BWANA akamwambia Shetani, "Tazama, yumo mkononi mwako; ni uhai wake tu
ambao lazima uutunze." 7 Kisha Shetani akatoka mbele ya uso wa BWANA. Akampiga
Ayubu na majipu mabaya toka wayo wa mguu hadi kichwani. 8 Ayubu akachukua
kipande cha kigae kujikunia, na akaketi chini majivuni. 9 Kisha mkewe akamuuliza,
"Je hata sasa wewe unashikamana na utimilifu wako? Umkufuru Mungu na ufe.
10 Lakini yeye akamwambia, "Wewe unaongea kama mmoja wa hao wanawake
wapumbavu waongeavyo. Je sisi tupate mema toka kwa Mungu na tusipate mabaya?"
Katika mambo hayo yote, Ayubu hakutenda dhambi kwa midomo yake. 11 Sasa
wakati rafiki zake watatu wa Ayubu walipopata habari ya mabaya yaliyompata,
kila mmoja wao akaja kutoka mahali pake: Elifazi Mtemani, Bildadi Mshuhi, na
Sofari Mnaamathi. Wakatenga muda ili waende kuomboleza naye na kumfariji.
12 Walipoinua macho yao wakiwa mbali, hawakuweza kumtambua. Wakapaza sauti
zao na kulia; kila mmoja wao akararua joho lake na kurusha majivu hewani na juu ya
kichwa chake. 13 Kisha wakaketi chini pamoja naye kwa muda wa siku saba-mchana
na usiku. Hakuna hata mmoja aliyesema naye neno, kwa kuwa waliona kuwa huzuni
yake ilikuwa kuu mno.

# 3

1 Baada ya hayo, Ayubu akafunua kinywa chake na kuilani siku aliyozaliwa.
2 Akasema, 3 "Na ipotelee mbali siku niliyozaliwa mimi, usiku uliosema, 'Mimba ya
mtoto wa kiume imetungwa.' 4 Siku hiyo na iwe giza; Mungu toka juu asiifikilie,
wala mwanga usiiangazie. 5 Ishikwe na giza na giza la mauti liwe lake. Wingu
na likae juu yake; kila kitu kiifanyacho siku kuwa giza kweli na kiitishe. 6 Usiku
huo, na ukamatwe na giza tororo. Usihesabiwe miongoni mwa siku za mwaka;
na usiwekwe katika hesabu ya miezi. 7 Tazama, usiku huo na uwe tasa; na sauti
ya shangwe isiwe ndani yake. 8 Na wailani siku hiyo, hao wafahamuo namna ya
kumuamsha lewiathani. 9 Nyota za mapambazuko yake zitiwe giza. Siku hiyo iutafute
mwanga, lakini isiupate; wala makope ya mapambazuko isiyaone, 10 kwasababu
haikuifunga milango ya tumbo la mama yangu, na kwasababu haikunifichia taabu
machoni pangu. 11 Kwanini si-kufa wakati lipotokeza katika tumbo la uzazi? Kwanini
sikuitoa roho yangu hapo mama aliponizaa? 12 kwanini magoti yake yalinipokea?
Kwanini maziwa yake yanipokee hata ninyonye? 13 Kwa sasa ningelikuwa nimelala
chini kimya kimya. Ningelala usingizi na kupata pumziko 14 pamoja na wafalme na
washauri wa dunia, ambao walijijengea makaburi ambayo sasa ni magofu. 15 Au
Ningelikuwa nimelala pamoja na wakuu wenye dhahabu, waliozijaza nyumba zao
fedha. 16 Au pengine ningekuwa sijazaliwa, kama watoto wachanga wasio uona
mwanga kabisa. 17 Huko waovu huacha kusumbua; huko waliochoka hupumzika.
18 Huko wafungwa kwa pamoja hupata amani; hawaisikii sauti ya msimamizi wa

watumwa. [19] Wote wadogo na watu maarufu wako huko; mtumishi yuko huru
kwa bwana wake huko. [20] Kwa nini yeye aliye mashakani kupewa mwanga?
Kwa nini hao wenye uchungu moyoni kupewa uhai, [21] ambao hutamani mauti
lakini hawapati; ambao huyachimbulia mauti zaidi ya kutafuta hazina iliyofichika?
[22] Kwa nini kupewa mwanga ambao hushangilia mno na kufurahi walionapo kaburi?
[23] Kwanini kupewa mwanga mtu ambaye njia zake zimefichika, mtu ambaye Mungu
amemzungushia uwa? [24] Kwa kuwa kushusha kwangu pumzi kwatokea badala ya
kula; kuugua kwangu kumemiminika kama maji. [25] Maana jambo lile niliogopalo
limenipata; nalo linitialo hofu limenijilia. [26] Mimi sioni raha, sipati utulivu, na sipati
pumziko; badala yake huja taabu."

# 4

[1] Kisha Elifazi Mtemani akajibu na kusema, [2] Kama mtu yeyote akijaribu
kuzungumza na wewe, je utakosa ustahimilivu? Lakini ni nani anaweza kujizuia
asizungumze? [3] Tazama, wewe umewafunza wengi; wewe imeipa nguvu mikono
iliyokuwa dhaifu. [4] Maneno yako yamemsaidia yeye mwanamme aliyekuwa
anaanguka; wewe umeyaimarisha magoti dhaifu. [5] Lakini sasa matatizo yamekuja
kwako, na wewe umechoka; yanakugusa wewe, na wewe umetatizika. [6] Je si hofu
yako imani yako, na ukamilifu wa njia zako tumaini lako? [7] Tafakari juu ya hili,
tafadhari: ni nani aliyeangamia akiwa hana kosa? Au ni lini watu wakamilifu
walikatiliwa mbali? [8] Kutokana na vile nilivyoona, wale walimao uovu na kupanda
taabu huvuna hayo. [9] Kwa pumzi ya Mungu huangamia; kwa mlipuko wa hasira
zake huteketea. [10] Kuunguruma kwa simba, sauti ya simba mkali, meno ya simba
wadogo - yamevunjika. [11] Simba mzee huangamia kwa kukosa wahanga; watoto
wa simba jike wametawanyiko kila mahali. [12] Sasa nililetewa kwangu jambo fulani
kisiri, na sikio langu likapokea uvumi kuhusu hilo. [13] Kisha yakaja mawazo kupitia
ndoto wakati wa usiku, wakati uwaangukiwapo usingizi mzito watu.. [14] Ilikuwa usiku
wakati nilipopatwa hofu na kutetemeka, na mifupa yangu yote ikatikisika. [15] Kisha
nafsi ikapita mbele ya uso wangu, na nywele zangu za mwili zilisimama. [16] Nafsi
ilisimama kimya, lakini sikuweza kupambanua sura yake. Umbo lilikuwa mbele
ya macho yangu; kulikuwa kimya, nami nikasikia sauti ikisema, [17] "Je binadamu
anaweza kuwa mwenye haki zaidi kuliko Mungu? Je mtu anaweza kuwa msafi zaidi
kuliko muumba wake? [18] Tazama, kama Mungu hawaamini watumishi wake; kama
hulaumu upumbavu wa malaika zake, [19] je si zaidi sana ukweli huu kwa wale waishio
katika nyumba za udongo, ambao misingi yao ipo katika vumbi, wale waliopondwa
mbele ya nondo? [20] Kati ya asubuhi na jioni wameangamizwa; wameangamia milele
wala bila yeyote kuwatambua. [21] Je kamba za hema yao hazikung'olewa kati yao?
Wanakufa; wanakufa bila hekima.

# 5

[1] Ita sasa; je kuna yeyote ambaye atakujibu? Utamrudia yupi katika watakatifu
hao? [2] Kwa kuwa hasira huua mtu mpumbavu; wivu huua mjinga. [3] Nimemuona mtu
mpumbavu akishika mzizi, lakini ghafla niliyalaani makazi yake. [4] Watoto wake wako
mbali na uzima; wameangamia langoni mwa mji. Hakuna yeyote atakaye waponya.
[5] Mwenye njaa hula mavuno yao; hata huyachukua katikati ya miiba. Wenye kiu
huzihemea mali zao. [6] Kwa kuwa magumu hayatoki udongoni; wala taabu haichipuki
katika nchi. [7] Badala yake, wanadamu huzaliwa kwaajili ya taabu, kama tu cheche
za moto zirukavyo juu. [8] Lakini kwa mimi, ningemrudia Mungu mwenyewe; kwake
ningeaminisha kusudi langu - [9] yeye afanyae makuu na mambo yasiyochunguzika,
mambo ya ajabu yasiyo na hesabu. [10] Hutoa mvua juu ya nchi, na huyapeleka

maji mashambani. [11] Hufanya haya kwaajili ya kuwainua juu hao walio chini;
huwapandisha sehemu salama hao waombolezao. [12] Yeye huharibu mipango ya watu
wenye hila, ili mikono yao isipate mafanikio. [13] Yeye huwanasa watu wenye hekima
katika matendo ya hila zao wenyewe; mipango ya watu waliogeuzwa huharibika
haraka. [14] Wao hupatwa na giza wakati wa mchana, na hupapasa mchana kama vile
ni usiku. [15] Lakini yeye huokoa maskini kwa upanga wa vinywa vyao na mhitaji kwa
mkono wa mtu mwenye nguvu. [16] Hivyo mtu maskini ana matumaini, na udhalimu
hufumba kinywa chake mwenyewe. [17] Tazama, amebarikiwa mtu ambaye hutiwa
adabu na Mungu; kwa sababu hiyo, usidharau uongozi wa Mwenyezi. [18] Kwa kuwa
yeye hujeruhi na kisha huuguza; yeye hutia jeraha na kisha mikono yake huponya.
[19] Yeye atakuokoa na mateso sita; kweli, katika mateso saba, hakuna uovu utakao
kugusa. [20] Wakati wa njaa atakukomboa na kifo, na kwa uwezo wa upanga wakati wa
vita. [21] Wewe utafichwa na mateso ya ulimi; na usitishike na uharibifu utakapokuja.
[22] Wewe utaufurahia uharibifu na njaa, na hutatishika na wanyama wakali wa
nchi. [23] Kwa kuwa wewe utakuwa na mapatano na mawe ya shambani mwako,
na wanyama wa mwituni watakuwa na amani na wewe. [24] Wewe utajua kwamba
hema lako lina usalama; utatembelea zizi la kondoo wako na hutakosa kitu chochote.
[25] Pia utafahamu kwamba uzao wako utakuwa mwingi, na vizazi vyako vitakuwa
kama nyasi ardhini. [26] Wewe utafika kaburini kwako mwenye umri kamili, kama vile
rundo la mashuke ya nafaka liendavyo juu wakati wake. [27] Tazama, tumelipeleleza
jambo hili; ndivyo lilivyo; lisikie, na ulifahamu kwa ajili yako mwenyewe."

# 6

[1] Kisha Ayubu akajibu na kusema, [2] "Oo, laiti maumivu yangu makubwa
yangepimwa; laiti misiba yangu yote mikubwa ingewekwa kwenye mizani! [3] Kwa
kuwa sasa ungekuwa mzito kuliko mchanga wa baharini. Kwa sababu hiyo maneno
yangu yamekuwa ya haraka. [4] Kwa kuwa mishale ya Mwenyezi ipo ndani yangu,
moyo wangu umelewa sumu; Vitisho vya Mungu vimejipanga vyenyewe dhidi yangu.
[5] Je punda mwitu hulia akiwa na malisho? Au ng'ombe huwa dhaifu wakati wa
njaa ambapo anachakula? [6] Je inawezekana kitu kisicho na ladha kulika bila
chumvi? Au kuna radha yoyote katika ute mweupe wa yai? [7] Nakataa kuvigusa;
kwangu mimi vinafanana na chakula kichukizacho. [8] Oo, kama nigeweza kupata
haja yangu; oo, kama Mungu angeridhia jambo nilitamanilo sana: [9] kama Mungu
ingempendeza kuniangamiza mara moja, kwamba angeulegeza mkono wake na
kuyakatilia mbali maisha yangu! [10] Hii ingeweza kuwa faraja yangu hata sasa - hata
kama nafurahia sana maumivu yasiyopungua: kwa kuwa sikuyakana maneno yake
Mtakatifu. [11] Nguvu yangu ni ipi, hata nijaribu kusubiri? Mwisho wangu ni upi,
utakao refusha maisha yangu? [12] Je nguvu zangu ni nguvu za mawe? Au mwili wangu
umeumbwa kwa shaba nyeusi? [13] Je si kweli kwamba sina msaada ndani yangu, na
kwamba hekima imeondolewa mbali nami? [14] Kwa mtu ambaye yu karibu kuzirai,
inapasa uaminifu uonyeshwe na rafiki zake; hata kwake yeye aachaye kumcha
Mwenyezi. [15] Lakini ndugu zangu wamekuwa waaminifu kwangu kama mkondo
wa maji jangwani, mfano wa mifereji ya maji ipitayo mpaka pasipo kitu, [16] ambayo
imekuwa mieusi kwa sababu ya barafu juu yake, na kwa sababu ya theluji ambayo
hujificha yenyewe ndani yake. [17] Wakati zikiyeyuka, hutoweka; kukiwa na joto,
hutoweka mahali hapo. [18] Misafara ambayo husafiri kwa njia yao hugeuka na maji;
huzurura jangwani na kisha hupotea. [19] Misafara kutoka Tema huitazama, wakati
majeshi ya Sheba huitarajia. [20] Wamevunjika moyo kwa sababu walitumaini kupata
maji. Wakaenda huko, lakini walidanganywa. [21] Kwa sasa ninyi rafiki si kitu kwangu;
mmeona hali yangu ya kutisha nanyi mwaogopa. [22] Je nilisema kwenu, 'Nipeni kitu

furani?' Au, 'nitoleeni zawadi katika mali zenu?' 23 Au, 'Niokoeni toka mkononi mwa
mtesi wangu?' Au, 'Nitoleeni fidia kwa watesi wangu?' 24 Nifundishe, nami nitaishika
amani yangu; nifanye nifahamu wapi nilipokosea. 25 Jinsi gani maneno ya kweli
yanavyo umiza! Lakini hoja zenu, jee hasa zimenionya nini mimi? 26 Je mnapanga
kuyakemea maneno yangu, mnayachukulia maneno ya mtu mwenye kukata tamaa
sawa na upepo? 27 Hasa, mna piga kura kwa ajili ya yatima, na kupatana bei juu ya
rafiki yenu kama bidhaa. 28 Sasa, kwa sababu hiyo, tafadhari nitazame, kwa hakika
sitasema uongo usoni penu. 29 Rudini, nawasihi; lisiwepo neno la uonevu na nyinyi;
Hasa, rudini, sababu zangu ni za haki. 30 Je mna uovu ulimini mwangu? Je kinywa
changu hakiwezi kungundua madhara?

# 7

1 Je mtu hana kazi ngumu juu ya nchi? Je siku zake si kama siku za mwajiriwa?
2 Kama mtumwa atamaniye sana kivuli cha jioni, kama mwajiriwa atafutaye ujira
wake - 3 hivyo nami nimeumbwa kuvumilia miezi ya taabu; Nami nimepewa taabu -
zimeujaza usiku. 4 Hapo nilalapo chini, najiuliza mwenyewe, 'Lini nitatoka kitandani
na lini usiku utatoweka?' Nimejawa na kujitupa huku na huko hadi mwanzo wa
siku. 5 Mwili wangu umevikwa minyoo na madonda yenye vumbi; maumivu katika
ngozi yangu yamekuwa magumu na kisha hutoweka na huendelea tena. 6 Siku
zangu zinakimbia kuliko chombo cha kufumia; zinapita bila tumaini. 7 Mungu,
anakumbuka kwamba maisha yangu ni pumzi tu; jicho langu halitaona mema tena.
8 Jicho lake Mungu, huyo anionaye mimi, halitaniangalia tena; Macho ya Mungu
yatanitazama, lakini sitakuwako. 9 kama vile wingu liishavyo na kutoweka, hivyo
wale waendao sheoli hawatarudi tena kabisa. 10 Yeye hatarudi tena nyumbani kwake,
wala mahali pake hapatamtambua tena. 11 Kwa sababu hiyo sitakizuia kinywa
changu; Nitasema juu ya maumivu makubwa ya roho yangu; Nitanung'unika juu
ya uchungu wa nafsi yangu. 12 Je mimi ni bahari au kiumbe cha kutisha baharini
hata ukaweka mlinzi juu yangu? 13 Hapo nisemapo, 'kitanda changu kitanifariji, na
malazi yangu yatatuliza manung'uniko yangu,' 14 halafu unitishapo kwa ndoto na
kunitisha kwa maono, 15 ili nichague kunyongwa na kufa kuliko kulinda mifupa
yangu hii. 16 Ninayachukia kabisa maisha yangu; sitamani siku zote kuwa hai;
usinisumbue maana siku zangu hazifai. 17 Je mtu ni nini hata ukatia bidii kwake,
na ukaweka akili yako kwake, 18 na kumwangalia kila asubuhi, na kumjaribu kila
mara? 19 Je itachukuwa muda gani kabla hujaacha kuniangalia, wala kunisumbua
muda wa kutosha kwaajili ya kumeza mate yangu? 20 Hata kama nimefanya dhambi,
itakusaidia nini, wewe ulindaye wanadamu? Kwa nini umenifanya shabaha yako,
kiasi kwamba nimekuwa mzigo kwako? 21 Kwa nini hunisamehi makosa yangu na
kuniondolea uovu wangu? kwa kuwa sasa nitalala mavumbini; na wewe utanitafuta
kwa bidii, lakini sitakuwako."

# 8

1 Kisha Bildadi huyo Mshuhi akajibu na kusema, 2 "hata lini wewe utasema mambo
haya? Kwa muda gani maneno ya kinywa chako yatakuwa kama upepo wenye
nguvu? 3 Je Mungu hupotosha hukumu? Je Mwenyezi hupotosha haki? 4 Watoto wako
wametenda dhambi dhidi yake; tunalifahamu hili, kwa kuwa amewatia mkononi kwa
makosa yao. 5 Lakini wewe unaonaje ukimtafuta Mungu kwa bidii na kufikisha haja
yako kwa huyo Mwenyezi. 6 Ukiwa wewe ni msafi na mkamilifu, hakika angeamka
mwenyewe kwa niaba yako na kukurudisha kwenye makazi ya haki yako. 7 Japokuwa
huo mwanzo wako ulikuwa ni mdogo, hata hivyo hali yako ya mwisho itaongezeka
sana. 8 Tafadhari uwaulize vizazi vya zamani, na utie bidii katika hayo mababu zetu

waliyojifunza. [9] (Sisi ni wa jana tu na hatujui chochote kwa kuwa siku zetu duniani ni
kivuli). [10] Je hawatakufunza wao na kukuambia? Je hawatatamka maneno yatokayo
mioyoni mwao? [11] Je hayo mafunjo yaota pasipo matope? Je mafunjo yaota pasipo
maji? [12] Wakati yakiwa bado ya kijani na hayajakatwa, hunyauka kabla ya mmea
mwingine. [13] Hivyo pia njia ya wote wamsahauo Mungu, na matumaini ya asiyeamini
Mungu yatatoweka. [14] Ujasiri wake utavunjika, na matumaini yake ni dhaifu kama
utando wa buibui. [15] Ataitegemea nyumba yake, lakini haitamsaidia; atashikamana
nayo, lakini isidumu. [16] Yeye huwa mti mbichi chini ya jua, na machipukizi yake
huenea katika bustani yake yote. [17] Mizizi yake hujifunga funga kwenye rundo la
mawe; huangalia mahali pazuri katikati ya mawe; [18] Lakini mtu huyu aking'olewa
mahali pake, kisha mahali pale patamkana, na kusema, 'mimi sikukuona.' [19] Tazama,
hii ni “furaha” ya mtu mwenye tabia hiyo; mimea mingine itachipuka toka katika
udongo ule ule mahali pake. [20] Tazama, Mungu hatamtupa mtu asiye na kosa; wala
hatawathibitisha watendao uovu. [21] Yeye atakijaza kinywa chako na kicheko, midomo
yako na shangwe. [22] Wale ambao wanakuchukia wewe watavishwa aibu; nayo hema
yake mwovu haitakuwepo tena.

# 9

[1] Kisha Ayubu akajibu na kusema, [2] “kweli najua kwamba ndivyo hivyo. Lakini
ni kwa namna gani mtu anakuwa na haki kwa Mungu? [3] Kama akitaka kujibishana
na Mungu, hatamjibu yeye mara moja katika elfu zaidi. [4] Mungu ni mwenye hekima
moyoni na ukuu katika nguvu; ni nani daima aliyejifanya mwenyewe kuwa mgumu
dhidi yake na akafanikiwa? - [5] ambaye huiondoa milima bila kumtahadharisha
yeyote wakati akiipindua katika hasira zake - [6] ambaye huitikisa nchi itoke mahali
pake na mihimili yake hutikisika. [7] Ni Mungu yule yule ambaye huliamuru jua
lisichomoze, nalo halichomozi, na ambaye huzihifadhi nyota, [8] ambaye peke yake
ni mwenye kupanua mbingu na kuyatuliza mawimbi ya bahari, [9] ambaye huumba
Dubu, Orioni, kilima, na makundi ya nyota ya kusini. [10] Ni Mungu yule yule atendaye
mambo makuu, mambo yasiyofahamika - hasa, mambo ya ajabu yasiyohesabika.
[11] Tazama, huenda karibu nami, na siwezi kumuona yeye; pia hupita kwenda mbele,
lakini ni simtambue. [12] Kama akichukua kitu chochote, nani atamzuia? Nani awezaye
kumuuliza, 'unafanya nini?' [13] Mungu hataondoa hasira yake; wamsaidiao Rahabu
huinama chini yake. [14] Je ni upungufu kiasi gani mimi nitamjibu, je nichague maneno
kuhojiana naye? [15] Hata kama ni mwenye haki, nisingelimjibu; ningeomba msamaha
tu kwa hukumu yangu. [16] Hata kama ningelimwita na yeye akanitikia, nisingeamini
kuwa ameisikia sauti yangu. [17] kwa kuwa yeye anidhoofishaye kwa dhoruba na
kuyaongeza majeraha yangu pasipo sababu. [18] Yeye hataki hata kuniruhusu nipate
kuvuta pumzi; badala yake, hunijaza uchungu. [19] Kama ni habari ya nguvu, tazama!
yeye ni mwenye uwezo! Kama ni habari ya haki, ni nani atakaye mhukumu?
[20] Ingawa ni mwenye haki, kinywa changu mwenyewe kitanihukumu; na ingawa ni
mtakatifu, maneno yangu yatashuhudia kuwa ni mwenye kosa. [21] Mimi ni mtakatifu,
lakini siijali zaidi nafsi yangu; Naudharau uhai wangu mwenyewe. [22] Haileti tofauti
yoyote, kwa sababu hiyo nasema kwamba yeye huangamiza watu wasio na makosa
na waovu pia. [23] Kama hilo pigo likiua ghafla, yeye atafurahi mateso yake mtu asiye
na kosa. [24] Dunia imetiwa mkononi mwa watu waovu; Mungu hufunika nyuso za
waamuzi wake. kama si yeye hufanya, ni nani basi? [25] Siku zangu zinapita haraka
kuliko tarishi akimbiae; siku zangu zinakimbia mbali; wala hazioni mema mahali
popote. [26] Zinapita kama mashua zilizoundwa kwa mafunjo ziendazo kwa kasi, na
zinakasi kama tai ashukaye upesi katika mawindo yake. [27] Kama ni kisema kwamba
mimi nitasahau kuhusu manung'uniko yangu, kwamba nitaacha kuonyesha sura ya

huzuni na kuwa na furaha, 28 Mimi nitaziogopa huzuni zangu zote kwa sababu
nafahamu kuwa hutanihesabu kuwa sina hatia. 29 Nitahukumiwa; kwa nini, basi,
nitaabike bure? 30 Kama najiosha mwenyewe kwa maji ya theluji na kuitakasa
mikono yangu na kuwa safi zaidi, 31 Mungu atanitumbukiza shimoni, na nguo zangu
mwenyewe zitanichukia. 32 Kwa kuwa Mungu si mtu, kama mimi, kwamba naweza
kumjibu, hata tukaribiane katika hukumu. 33 Hakuna hakimu baina yetu awezaye
kuweka mkono wake juu yetu sote. 34 Hakuna hakimu mwingine ambaye anaweza
kuniondolea fimbo ya Mungu, awezaye kuzuia kitisho chake kisinitie hofu. kisha
ningesema na nisimuogope. 35 Lakini kama mambo yalivyo sasa, sitaweza kufanya
hivyo.

# 10

1 Nimechoka na maisha yangu; Nitanena wazi manung'uniko yangu; nitasema kwa
uchungu wa roho yangu. 2 Nitamwambia Mungu, 'Usinihukumie makosa; nionyeshe
sababu za wewe kunilaumu mimi. Je 3 ni vizuri kwako wewe kunionea mimi,
kudharau kazi ya mikono yako wakati unafurahia juu ya mipango ya waovu? 4 Je
wewe una macho ya kimwili? Je wewe unaona kama mtu aonavyo? 5 Je siku zako ni
kama siku za wanadamu au miaka yako ni kama miaka ya watu, 6 hata ukauliza
habari za uovu wangu na kuitafuta dhambi yangu, 7 ingawa wewe wafahamu
mimi sina kosa na hapana mwingine awezaye kuniokoa mimi na mkono wako?
8 Mikono yako imeniumba na kunifinyanga kwa wakati mmoja nawe kunizunguka,
hata hivyo unaniangamiza. 9 Kumbuka, nakuomba, ulivyonifinyanga kama vile
udongo; je utanirudisha mavumbini tena? 10 Je wewe hukunimimina kama maziwa
na kunigandisha mfano wa jibini? 11 Umenivika ngozi na nyama na kuniunganisha
pamoja kwa mifupa na misuli.. 12 Wewe umenizawadia mimi uhai na ahadi ya
upendeleo na usaidizi wako umeilinda roho yangu. 13 Hata hivyo mambo haya
uliyaficha moyoni mwako - nafahamu kwamba hivi ndivyo ufikirivyo: 14 kuwa kama
nimefanya dhambi, wewe utaizingatia; hutaniachilia na uovu wangu. 15 Kama mimi
ni muovu, ole wangu; hata kama ni mwenye haki, sitaweza kuinua kichwa changu,
kwa kuwa nimejaa aibu na kuyaangalia mateso yangu. 16 Kama kichwa changu
kikijiinua chenyewe, waniwinda kama simba; tena wajionyesha mwenyewe kuwa ni
mwenye nguvu kwangu. 17 Wewe unaleta mashahidi wapya dhidi yangu na kuzidisha
hasira zako dhidi yangu; wanishambulia na majeshi mapya. 18 Kwa nini, basi, ulinitoa
tumboni? Natamani ningekata roho na ili jicho lolote lisinione. 19 Ningelikuwa kama
asiyekuwepo; ningelichukuliwa kutoka tumboni mpaka kaburini. 20 Je si siku zangu
pekee ni chache? Acha basi, usinisumbue, ili kwamba nipate kupumzika kidogo
21 kabla sijaenda huko ambako sitarudi, kwenye nchi ya giza na kivuli cha mauti,
22 ni nchi ya giza kama usiku wa manane, nchi ya kivuli cha mauti, isiyokuwa na
mpangilio, ambayo nuru yake ni kama usiku wa manane.'”

# 11

1 Ndipo Sofari Mnaamathi alijibu na kusema, 2 “ Huo wingi wa maneno haupaswi
kujibiwa? Mtu huyu, aliyejaa maneno mengi awe wa kuaminiwa? 3 Kujivuna kwako
kunapaswa kuwafanya wengine wabaki wamenyamaza? Wakati unapoyadhihaki
mafundisho yetu, hakuna awaye yote atakayekufanya wewe ujisikie mwenye aibu?
4 Kwa kuwa wewe unasema kwa Mungu, 'Imani yangu ni safi, Mimi sina waa lolote
machoni pako.' 5 Lakini, laiti, Mungu huyo angesema na kufungua midomo yake
dhidi yako; 6 hivyo angekuonyesha wewe siri za hekima! Kwa kuwa yeye ni mkuu
katika ufahamu. Tena tambua huyo Mungu anataka kutoka kwako kidogo kuliko
uovu wako unavyostahili. 7 Je, wewe unaweza kumfahamu Mungu kwa kumtafuta

yeye? Unaweza kumtambua aliye mkuu kwa ukamilifu? 8 Upeo uko juu kama
mbingu; unaweza kufanya nini wewe? Ni wenye kina kirefu kuliko kuzimu; waweza
kufahamu nini wewe? 9 Vipimo vyake ni virefu kuliko nchi, na vipana kuliko bahari.
10 kama yeye akipita kati na kumyamazisha mtu yeyote, kama yeye akimwita mtu
yeyote hukumuni, tena ni nani anayeweza kumzuia yeye? 11 Kwa maana anawajua
watu waongo; wakati anapoona uovu, hawezi yeye kuukumbuka? 12 Lakini watu
wapumbavu hawana ufahamu; wataupata wakati punda mwitu atakapozaa mtu.
13 Lakini ikiwa umeuelekeza moyo wako kwa haki na umeunyosha mkono wako
karibu na Mungu; 14 ikiwa huo uovu ulikuwa katika mikono yako, lakini hivyo
tena unauweka mbali nawe, na haukuruhusu kutokuwa mwenye haki kukaa hemani
mwako. 15 Ndipo kwa hakika ungeinua juu uso wako bila ishara ya aibu; Ni dhahiri,
ungethibitika na usingeogopa. 16 Wewe ungesahau mateso yako; ungeyakumbuka
hayo tu kama maji ambayo yametiririka mbali. 17 Maisha yako yangekuwa angavu
kuliko adhuhuri; japokuwa kulikuwa na giza, litakuwa kama asubuhi. 18 Ungekuwa
salama kwa sababu kuna tumaini; ni dhahiri, wewe utapata usalama juu yako na
utachukua pumziko lako katika usalama. 19 Pia ungelala chini katika pumziko, na
hakuna ambaye angekufanya wewe uogope; hakika wengi wangetafuta upendeleo
wako. 20 Lakini macho ya watu waovu yatashindwa; hawatakuwa na njia ya
kukimbia; tumaini lao la pekee litakuwa pumzi yao ya mwisho ya uhai.

# 12

1 Ndipo Ayubu akajibu na kusema, 2 “Hakuna shaka ninyi wanadamu; Hekima
mtakufa nayo. 3 Lakini nina ufahamu kama vile ninyi; Mimi siyo duni kwenu. Ni
dhhiri, ni nani asiyefahamu vitu hivyo kama hivi? 4 Mimi ni kitu cha kuchekwa na
jirani-Mimi, ni mmoja aliyemwita Mungu na ambaye alijibiwa na yeye! Mimi, ni
mwenye haki na mtu asiyekuwa na hatia-Mimi sasa nimekuwa kitu cha kuchekwa.
5 Katika mawazo yake mtu fulani aliye katika kufurahi, kuna kudharau kwa mashaka;
hufikiri katika njia ambayo huleta mambo mabaya zaidi kwa wale ambao miguu
yao inateleza. 6 Hema za wezi hufanikiwa, na wale ambao humkasirisha Mungu
huhisi salama; mikono yao wenyewe ni miungu wao. 7 Lakini sasa waulize hao
wanyama wa mwituni, na watakufundisha wewe; waulize ndege wa angani, na
watakuambia wewe. 8 Au iambie ardhi, na itakufundisha wewe; samaki wa baharini
watakutangazia wewe. 9 Ni myama yupi miongoni mwa hawa asiyefahamu kuwa
mkono wa Yahwe umetenda haya? 10 Katika mkono wake mna uzima wa kila
kiumbe hai na pumzi ya wanadamu wote. 11 Je, sikio haliyajaribu maneno kama vile
kaakaa lionjavyo chakula chake? 12 Kwa wazee mna hekima; katika wingi wa siku
mna ufahamu. 13 Pamoja na Mungu mna hekima na ukuu; yeye anayo mashauri
na ufahamu. 14 Tazama, yeye huangusha chini, na haiwezekani kujengwa tena;
kama yeye akimtia gerezani mtu yeyote, hakutakuwa tena kufunguliwa. 15 Tazama,
kama yeye akiyazuia maji, yanakauka; na kama akiyaachilia nje yanaitaabisha
ardhi. 16 Pamoja na yeye mna nguvu na hekima; watu ambao wamedanganywa
na mdanganyi wote pamoja wako katika nguvu zake. 17 Yeye huwaongoza washauri
mbali bila kuvaa viatu katika huzuni; huwarudisha hakimu katika upumbavu. 18 Yeye
Huondoa minyororo ya mamlaka kutoka kwa wafalme; yeye hufunika viuno vyao
kwa nguo. 19 Yeye huwaongoza makuhani mbali bila kuvaa viatu na kuwapindua
watu wakuu. 20 Yeye huondoa hotuba ya wale waliokuwa wameaminiwa na huondoa
mbali ufahamu wa wazee. 21 Yeye humwaga aibu juu ya binti za wafalme na
hufungua mishipi ya watu wenye nguvu. 22 Yeye huweka wazi vitu vya kina kutoka
katika giza na kuvileta nje kumuika vivuli mahali ambapa watu waliokufa wapo.
23 Yeye huyafanya mataifa kuwa na nguvu, na pia huyaharibu; Yeye pia huyakuza

mataifa, na pia yeye huyaongoza mbali kama wafungwa. 24 Yeye huondoa mbali
ufahamu kutoka kwa viongozi wa watu wa nchi; huwafanya wao kutangatanga
msituni mahali pasipo na njia. 25 Wao wanapapasa katika giza bila kuwa na mwanga;
yeye huwafanya wao kuweweseka kama mtu mlevi.

## 13

1 Tazama, jicho langu limeyaona haya yote; sikio langu limeyasikia na kuyaelewa
hayo. 2 Kile mnachokifahamu, ndicho hicho mimi pia ninachokifahamu; Mimi
siyo duni kwenu ninyi. 3 Hata hivyo, Mimi ningeweza kuzungumza na mwenye
nguvu; Mimi natamani kusemezana na Mungu. 4 Lakini ninyi mnauficha ukweli
kwa uongo; ninyi nyote ni tabibu msiokuwa na thamani. 5 Laiti, kwamba kwa
pamoja mngeshikilia amani yenu! Hilo lingekuwa hekima yenu ninyi. 6 Sikia sasa
kuhoji kwangu; Sikiliza kusihi kwa midomo yangu mwenyewe. 7 Ninyi mtazungumza
visivyo haki kwa ajili ya Mungu, na ninyi mtazungumza udanganyifu kwa yeye?
Ni kweli ninyi mngeonyesha ukarimu kwa yeye? 8 Ni kweli ninyi mngetetea katika
mahakama kama mawakili wa Mungu? 9 Je, kweli ingekuwa vizuri kwenu wakati
yeye akiwatafuta ninyi? Mngeweza ninyi kumdanganya yeye kama mlivyoweza
kuwadanganya watu? 10 Yeye kwa hakika angewathibitisha upya ninyi ikiwa
katika siri ninyi mmeonyesha kutokukamilika. 11 Je, ukuu wake usingewafanya
ninyi muogope? Je, utisho wake usingeshuka juu yenu? 12 Hadithi zenu za
misemo ya kukariri, ni mithali zimetengenezwa kwa majivu; utetezi wenu ni utetezi
uliotengenezwa kwa udongo wa mfinyanzi. 13 Shikilieni amani yenu, mniache peke
yangu, ili ya kwamba nipate kusema, acheni yaje yale yanayoweza kuja kwangu.
14 Nitaichukua nyama yangu mwenywewe katika meno yangu; Nitayachukua maisha
yangu katika mikono yangu. 15 Tazama, ikiwa ataniua mimi, sitakuwa na tumaini
lililobakia; hata hivyo, nitazitetea njia zangu mbele zake yeye. 16 Hiki kitakuwa
sababu ya kutohesabiwa hatia, kwamba mimi sikuja mbele zake kama mtu asiyemcha
Mungu. 17 Mungu, sikiliza kwa makini kuzungumza kwangu; ruhusu kutangaza
kwangu kuje kwenye masikio yako. 18 Tazama sasa, Nimeuweka utetezi wangu
katika mpangilio, Mimi ninafahamu kwamba mimi sina hatia. 19 Ni nani anayeweza
kushindana na mimi katika mahakama? Ikiwa mlikuja kufanya hivyo, na kama
mimi nilithibitishwa kukosea, ndipo ningekuwa kimya na kuyatoa maisha yangu.
20 Mungu, fanya mambo mawili kwa ajili yangu, na tena Mimi sitajificha kutoka
katika uso wako. 21 Ondoa kutoka kwangu mkono wako unaotesa, na usiache utisho
wako unifanye mimi kuogopa. 22 Ndipo niite mimi, na mimi nitakujibu; au uniache
mimi niseme na wewe na wewe unijibu mimi. 23 Je, maovu yangu na dhambi zangu
ni ngapi? Nijulishe kosa langu na dhambi yangu. 24 Kwa nini unaficha uso wako
kutoka kwangu mimi na kunitendea mimi kama adui yako? 25 Je, wewe utalitesa
jani linalopeperushwa? Je, utaendelea kulifuatilia bua kavu? 26 Kwa maana wew
unaandika chini vitu vichungu dhidi yangu mimi; wewe unanifanya mimi kurithi
uovu wa ujana wangu. 27 Wewe pia unaiweka miguu yangu katika nguo nyembamba;
wewe waangalia njia zangu zote; wewe wachunguza chini mahali ambapo nyayo
za miguu yangu zimekanyaga. 28 japokuwa mimi ni kama kitu kilichooza ambacho
hutupwa mbali, kama vazi lile ambalo nondo wamelila.

## 14

1 Mwanadamu, ambaye amezaliwa na mwanamke, huishi siku chache tu na amejaa
mahangaiko. 2 Yeye huchanua kutoka katika ardhi kama ua na kukatwa chini; yeye
hukimbia kama kivuli na hawezi kudumu. 3 Je, wewe unatazama chochote katika
hivi? Mnanileta mimi hukumuni pamoja nanyi? 4 Ni nani anayeweza kukileta

kitu safi kutoka katika kitu kichafu? Hakuna awaye yote. [5] Siku za mwanadamu
zimeamriwa. Idadi ya miezi yake unayo wewe; umekiweka kikomo chake ambacho
hawezi kukivuka. [6] Tazama mbali kutoka kwake kwamba yeye aweze kupumzika, ili
kwamba aweze kufurahia siku yake kama mtu aliyekodishwa kama yeye anaweza
kufanya hivyo. [7] Kunaweza kuwa na tumaini kwa mti; kama ukikatwa chini, unaweza
kuchipua tena, hivyo chipukizi lake halitapotea. [8] Japokuwa mizizi yake inakua
na kuzeeka katika ardhi, na shina lake kufa katika udongo, [9] hata kama bado lina
harufu ya maji pekee, litachipua tena na kutoa nje matawi kama mche. [10] Lakini
mwanadamu hufa; yeye huwa dhaifu; haswaa, mwanadamu hukoma kupumua, na
tena yuko wapi yeye? [11] Kama maji yanavyopotea kutoka ziwani, na kama vile
mto upotezavyo maji na kukauka, [12] vivyo hivyo watu hulala chini na hawaamki
tena. Mpaka pale mbingu zitakapokuwa hazipo tena, hawataamka wala kuamshwa
kutoka katika kulala kwao. [13] Laiti, kwamba ungenificha mimi mbali katika kuzimu
mbali kutoka katika mahangaiko, na kwamba ungenitunza mimi katika siri hadi
hasira yake imalizike, kwamba ungeniwekea mimi muda maalumu wa kukaa huko
na kisha kuniita mimi katika fahamu! [14] Ikiwa mwanadamu akifa, yeye ataishi tena?
Ikiwa hivyo, ningependa kusubiri kule muda wangu wote wa kuharibika mpaka
kufunguliwa kwangu kutakapokuja. [15] Wewe ungeita, na mimi ningekujibu wewe.
Wewe ungekuwa na shauku ya kazi ya mikono yako. [16] Wewe ungehesabu na kutunza
nyayo zangu; Wewe usingejali kumbukumbu ya dhambi yangu. [17] Uovu wangu
ungetiwa muhuri katika mkoba; wewe ungeufunga uovu wangu. [18] Lakini hata
milima huanguka na kuwa si chochote; hata miamba huhamishwa kutoka mahali
pake; [19] maji yaliyokuwa chini ya mawe; kufurika kwake huondoa mbali mavumbi
ya nchi. Kama hivi, ninyi mnavyoharibu matumaini ya mwanadamu. [20] Ninyi daima
humshinda yeye, na yeye hupita mbali; Ninyi mnabadilisha uso wake na kumtuma
yeye mbali kufa. [21] Kama watoto wake wa kiume ni wa kuheshimiwa, yeye, hatambui
hicho; na kama wakishushwa chini, yeye haoni hicho. [22] Yeye hujisikia tu maumivu
ya mwili wake mwenyewe, na hujiombolezea yeye mwenyewe.

# 15

[1] Ndipo Elifazi Mtemani alijibu na kusema, [2] Mtu mwenye hekima anapaswa kujibu
kwa maarifa yasiyofaa na kujijaza mwenyewe na upepo wa mashariki? [3] Anapaswa
kuhojiana na mazungumzo yasiyo na faida au na hotuba ambazo kwa hizo yeye
hawezi kufanya mema? [4] Dhahiri, wewe wafifisha heshima ya Mungu; Wewe
wazuia heshima kwa yeye, [5] kwa maana uovu wako hufundisha midomo yako;
Wewe wachagua kuwa na ulimi wa mtu mwenye hila. [6] Mdomo wako mwenyewe
hukukukumu wewe, siyo wangu; hakika, midomo yako mwenyewe hushuhudia dhidi
yako wewe. [7] Je, wewe ni mwanadamu wa kwanza ambaye aliyezaliwa? Wewe
ulikuwepo kabla ya vilima kuwepo? [8] Wewe Umewahi kusikia maarifa ya siri
ya Mungu? Je, wewe wajihesabia mwenye hekima wewe mwenyewe? [9] Ni kitu
gani unachokifahamu wewe ambacho sisi hatukijui? Ni kitu gani unachokifahamu
wewe ambacho hakiko katika sisi? [10] Pamoja nasi wapo pia wenye mvi na watu
wazee sana ambao ni wazee zaidi kuliko baba yako. [11] Je, faraja ya Mungu ni
ndogo sana kwako, maneno ambayo ni ya upole dhidi yako wewe? [12] Kwa nini
moyo wako wewe unakupeleka mbali? Kwa nini macho yako yananga'ra, [13] ili ya
kwamba kuirejesha roho yako kwa Mungu na kuyatoa maneno hayo kutoka katika
mdomo wako? [14] Je, mwanadamu yeye ni nini kwamba yeye anapaswa kuwa safi?
Yeye mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke ni nini kwamba yeye anapaswa awe
mwenye haki? [15] Tazama, Mungu haweki tumaini lake hata kwa mmoja wake aliye
mtakatifu; Hakika, mbingu haziko safi machoni pake yeye; [16] jinsi gani asivyo safi ni

mmoja aliye mbaya na mla rushwa, mtu ambaye hunywa uovu kama maji! 17 Mimi
nitakuonyesha wewe; Nisikilize mimi; Mimi nitakutangazia wewe vitu ambavyo
nimeviona, 18 vitu ambavyo watu wenye hekima wamepita chini yake kutoka kwa
baba zao, vile vitu ambavyo mababu zao hawakuvificha. 19 Hawa walikuwa mababu
zao, ambao kwao pekee nchi walipewa, na miongoni mwao hakuna mgeni aliyepita.
20 Mtu mwovu hupitia katika maumivu siku zake zote, idadi ya miaka iliyowekwa
juu kwa mtesaji kuteseka. 21 Sauti ya vitisho katika masikio yake; pindi yeye yuko
katika kufanikiwa, mharibu atakuja juu yake yeye. 22 Yeye hafikiri kwamba yeye
atarudi kutoka katika giza; Upanga humngojea yeye. 23 Yeye huenda sehemu mbali
mbali kwa ajili ya mkate, akisema, 'Kiko wapi? ' Yeye anatambua kuwa siku ya giza
iko mkononi. 24 Dhiki na mateso makali humfanya aogope; wao hushinda dhidi yake
yeye, kama mfalme tayari kwa vita. 25 Kwa sababu yeye ameunyosha mkono wake
dhidi ya Mungu na ameishi kwa kiburi dhidi ya aliye mkuu, 26 huyu mtu mwovu
hukimbia kwa Mungu na shingo ngumu, kwa vifundo vikubwa vya ngao. 27 Hii
ni kweli, hata ingawa yeye amefunika uso wake kwa mafuta yake na amekusanya
mafuta juu ya viuno vyake, 28 na ameishi katika miji yenye ukiwa; katika nyumba
ambazo hakuna mwanadamu anayeishi humo sasa na ambazo zilikuwa tayari kuwa
magofu. 29 Yeye hatakuwa tajiri; utajiri wake yeye hautadumu; hata kivuli chake
hakitadumu katika nchi. 30 Yeye hatatoka nje ya giza; mwali wa moto utakausha
matawi yake; katika pumzi ya kinywa cha Mungu yeye ataenda zake. 31 Mwacheni
yeye asitumaini katika vitu visivyofanya kazi, akijidanganya yeye mwenyewe; maana
upuuzi utakuwa mshahara wake yeye. 32 Itatokea kabla ya wakati wake yeye
atapaswa kufa; tawi lake halitakuwa kijani. 33 Yeye atazipukutisha zabibu zake
zisizovunwa kama mzabibu; yeye atayaondoa maua yake kama mti wa mzeituni.
34 Kwa maana msaada wa watu wasiomcha Mungu utakuwa tasa; moto utateketeza
hema za rushwa. 35 Wao wanabeba mimba yenye ubaya na kuzaa uovu; tumbo lao
hutunga mimba ya udanganifu.

# 16

1 Ndipo Ayubu akajibu na kusema, 2 “Mimi nimevisikia vitu hivyo vingi; ninyi nyote
ni wafariji wenye kuhuzunisha. 3 Maneno yenye upuuzi daima yanaweza kuwa
na mwisho? Nini kimeharibika kwenu kwamba mnajibu kama hivi? 4 Mimi pia
ningeweza kuzungumza kama ninyi mnavyofanya, kama ninyi mngekuwa katika
nafasi yangu; Mimi ningekusanya na kuunganisha maneno pamoja dhidi yenu
na kutikisa kichwa changu kwenu ninyi katika dhihaka. 5 Laiti, jinsi gani Mimi
ningewatia moyo na midomo yangu! Jinsi gani faraja kutoka midomo yangu
ingenga'risha huzuni yenu! 6 Ikiwa Mimi ninazungumza, kuomboleza kwangu
hakujasikilizwa; Ikiwa nikiendelea katika kuzungumza, jinsi gani mimi ninaidiwa?
7 Lakini sasa, Mungu, 8 wewe umenifanya mimi kuchoka; wewe umeifanya familia
yangu yote kuwa ukiwa. Wewe umenifanya mimi kukauka, ambayo yenyewe ni
ushuhuda dhidi yangu mimi; kukonda kwa mwili wangu huinuka dhidi yangu, na
kunashuhudia dhidi ya macho yangu. 9 Mungu amenirarua mimi katika ghadhabu
yake na amenitesa mimi; Yeye amenisaga mimi kwa meno yake; Adui yangu
amenikazia macho yake juu yangu kama yeye anavyonirarua mimi vipande. 10 Watu
wameachama na midomo iliyowazi juu yangu; wamenipiga mimi katika shavu kwa
kunitukana; wamekusanyika pamoja kinyume changu mimi. 11 Mungu amenikabidhi
mimi juu ya watu wasio mcha Mungu, na kunitupa mimi ndani ya mikono ya watu
waovu. 12 Mimi nilikuwa katika wepesi, na yeye amenivunjavunja mimi vipande.
Hakika, amenichukua mimi kwa shingo na ameniponda mimi vipande vipande;
yeye pia ameniweka mimi juu kama shabaha yake. 13 Wapiga upinde wake wote

wamenizunguka mimi; Mungu huzikata vipande vipande figo zangu, na haniokoi
mimi; yeye humwaga nje nyongo yangu juu ya ardhi. 14 yeye hukanyaga kanyaga
kupitia ukuta wangu tena na tena; yeye hukimbia juu yangu mimi kama shujaa.
15 nguo ya magunia juu ya ngozi yangu; Mimi nimeisukuma kwa nguvu pembe
yangu ndani ya ardhi. 16 Uso wangu ni mwekundu na kuomboleza; juu ya ngozi
inayofunika macho kuna kivuli cha mauti 17 ingawa hakuna dhuluma katika mikono
yangu, na kuomba kwangu ni safi. 18 Nchi, haifuniki juu damu yangu mimi; acha
kulia kwangu kuwe hakuna mahali pa kupumzika. 19 Hata sasa, tazama, ushuhuda
wangu uko mbinguni; yeye ambaye ashuhudiaye kwa ajili yangu mimi yuko juu.
20 Rafiki zangu wananicheka kwa dharau, lakini jicho langu linamwaga machozi kwa
Mungu. 21 Mimi ninaomba ule ushuhuda ulioko mbinguni kumtetea mtu huyu na
Mungu kama mwanadamu afanyavyo na jirani yake. 22 Kwa maana wakati miaka
michache itakapokuwa imepita, Mimi nitakwenda mahali ambapo mimi sitaweza
kurudi.

# 17

1 Roho yangu imemezwa, na siku zangu zimekwisha; kaburi lipo tayari kwa ajili
yangu mimi. 2 Hakika kuna wenye mzaha pamoja nami; ni lazima daima jicho
langu litazame kukasirisha kwao. 3 Nipe sasa ahadi, uwe uthibitisho kwangu mimi
pamoja na wewe mwenyewe; nani mwingine yuko pale ambaye atanisaidia mimi?
4 Kwa kuwa wewe Mungu umemeitunza mioyo yao kutoka katika ufahamu; kwa
hiyo, wewe hautawaheshimisha wao juu yangu mimi. 5 Yeye ambaye huwapinga
rafiki zake hadharani, kwa ajili ya tuzo, macho ya watoto wake yatashindwa kuona.
6 Lakini amenifanya mimi kuwa neno la kuzungumziwa na watu; wao wananitemea
mate katika uso wangu mimi. 7 Jicho langu pia halioni vizuri kwa sababu ya
huzuni; sehemu zangu zote za mwili ni nyembamba kama vivuli. 8 Watu wanyoofu
watapendezwa na hiki; mtu asiye na hatia atajitia yeye mwenyewe juu ya kushindana
dhidi ya watu wasiomcha Mungu. 9 Mtu mwenye haki ataendelea katika njia
yake; yeye ambaye ana mikono iliyo safi ataendelea kuwa mwenye nguvu zaidi na
zaidi. 10 Lakini kama ilivyo kwenu ninyi nyote, njooni sasa; Mimi sitampata mtu
mwenye hekima miongoni mwenu ninyi. 11 Siku zangu zimepita; mipango yangu
imenyamazishwa na hivyo ni matumaini ya moyo wangu. 12 Watu hawa, wenye
kukejeli, badili usiku kuwa mchana; mchana uko karibu kuwa giza. 13 Tangu mimi
nitazame katika Kuzimu kama nyumbani kwangu; tangu Mimi nimetandaza kiti
changu katika giza; 14 tangu Mimi nimesema na shimo 'Wewe ni baba yangu,' na kwa
funza, 'Wewe ni mama yangu au dada yangu; 15 liko wapi tena tumaini langu? Kama
kwa tumaini langu, nani awezaye kuona chochote? 16 Tumaini litakwenda pamoja
na mimi katika milango ya Kuzimu wakati sisi tutakapokwenda katika mavumbi?

# 18

1 Ndipo Bildadi Mshuhi alijibu na kusema, “ 2 Je, lini utaacha kusema kwako?
Fikiri, na baadaye tutazungumza. 3 Kwa nini sisi tumehesabiwa kama wanyama
mwitu; kwa nini tumekuwa wapumbavu machoni pako? 4 Wewe ambaye wajirarua
mwenyewe katika hasira yako, nchi haipaswi kuachwa kwa ajili yako au miamba
inapaswa kuondolewa kutoka mahali pake? 5 Ni dhahiri, nuru ya watu waovu
itawekwa nje; cheche ya moto wake haitanga'ra. 6 Nuru itakuwa giza katika hema
yake; taa yake juu yake yeye itawekwa nje. 7 Hatua za nguvu zake yeye zitafanywa
kuwa fupi; mipango yake yeye mwenyewe itamwangusha yeye chini. 8 Kwa maana
yeye atatupwa katika mtego kwa miguu yake mwenyewe; yeye atatembea katika
mahangaiko. 9 Tanzi litamchukua yeye kwa kisigino; mtego utabaki kushikilia juu

yake. 10 Tanzi limefichwa kwa ajili yake chini ya ardhi; na mtego kwa ajili yake katika
njia. 11 Watishao watamfanya yeye aogope juu ya sehemu zote; wao watamkimbiza
yeye kwenye visigino vyake. 12 Utajiri wake utageuka kuwa njaa, na majanga
yatakuwa tayari upande wake. 13 Sehemu za mwili wake zitakuwa zimemezwa;
Hakika, mzaliwa wa kwanza wa kifo atazila sehemu zake yeye. 14 Yeye ameraruliwa
kutoka kwenye usalama wa hema yake na hakuweza kutembea kwenda kwa mfalme
mwenye utisho. 15 Watu ambao siyo wa kwake wataishi kwenye hema yake baada
ya kuona ule moto mesambaa ndani ya nyumba yake yeye. 16 Mizizi yake itanyauka
chini yake; juu tawi lake yeye litakatwa. 17 Kumbukumbu lake yeye litapotea kutoka
katika nchi; yeye hatakuwa na jina katika mtaa. 18 Yeye atafukuzwa kutoka katika
nuru mpaka kwenye giza na kuwa amefukuzwa nje na ulimwengu huu. 19 Hatakuwa
na mtoto wa kiume wala mjukuu miongonni mwa watu wake, wala kizazi chochote
kitakachobakia mahali alipokuwa amekaa. 20 Wale wanaoishi upande wa magharibi
watakuwa wametiwa hofu kwa kile kitakachotokea kwake siku moja; wale wanaoishi
upande wa mashariki watakuwa wameogopeshwa kwa hicho. 21 Hakika hizo ni
nyumba za watu wasio haki, ni sehemu ya wale wasiomjua Mungu.”

## 19

1 Ndipo Ayubu akajibu na kusema, 2 lini mtanifanya mimi kuteseka na kunivunja
vunja mimi vipande vipnde kwa maneno? 3 Mara kumi hivi mmenishutumu mimi;
ninyi hamuoni aibu kwamba mmenitendea mimi kwa ukatili. 4 Kama ni dhahiri
kweli mimi nimekosa, makosa yangu hubaki kuwa wajibu wangu. 5 Kama ni
dhahiri ninyi mtajiinua juu yangu mimi na kuutumia uvumilivu wangu kunipinga
mimi, 6 kisha ninyi mnapaswa kutambua kwamba Mungu amefanya mabaya kwangu
mimi na amenikamata mimi katika mtego wake yeye. 7 Tazama, Mimi ninalia kwa
sauti, “dhuluma!” lakini sipati jibu. Mimi ninaita kwa ajili ya msaada, lakini
hakuna haki. 8 Yeye ameiwekea ukuta njia yangu, ili kwamba mimi nisiweze
kupita, na yeye ameweka giza katika njia yangu. 9 Yeye ameniondoa Mimi kutoka
katika utukufu wangu, na ameichukua taji kutoka kwenye kichwa changu mimi.
10 Yeye amenivunjavunja mimi chini kwa kila upande, na Mimi nimetoweka; yeye
amelikokota juu tumaini langu kama mti. 11 Yeye pia ameiongeza ghadhabu yake
dhidi yangu mimi; yeye ananihesabu mimi kama mmoja wa adui zake. 12 Majeshi
yake huja juu pamoja; wao wananikosesha tumaini kwa kuniteka nyara kwa kundi
kubwa kupigana na mimi wakizunguka hema yangu. 13 Yeye amewaweka ndugu
zangu mbali kutoka kwangu mimi; watu wangu wa karibu wote wamejitenga kutoka
kwangu mimi. 14 Vizazi vyangu vimeniangusha mimi; rafiki zangu wa karibu
wamenisahamu mimi. 15 Wale ambao mwanzoni walikaa kama wageni ndani ya
nyumba yangu na watumishi wangu wa kike, hunihesabu mimi kama mgeni. Mimi
nimekuwa mgeni katika macho yao. 16 Mimi ninamwita mtumishi wangu, lakini
yeye hanipi jibu japokuwa Mimi nimemsihi yeye kwa midomo yangu. 17 Pumzi yangu
mimi ni chukizo kwa mke wangu; Hata mimi ninachukiwa na wale ambao walizaliwa
kutoka katika tumbo la mama yangu mimi. 18 Hata watoto wachanga wananichukia
mimi; ikiwa Mimi nitainuka kuzungumza, wao huzungumza dhidi yangu mimi.
19 Rafiki zangu wote ninaowazoea wananichukia sana mimi; wale ambao Mimi
ninawapenda wamegeuka kinyume na mimi. 20 Mifupa yangu inashikamana kwenye
ngozi yangu na kwenye mwili wangu; Mimi ninaishi tu kwa ngozi ya meno yangu.
21 Iweni na huruma juu yangu mimi, muwe na huruma juu yangu mimi, rafiki
zangu, kwa maana mkono wa Mungu umenigusa mimi. 22 Kwa nini mnanitesa
mimi kama ninyi mlikuwa Mungu? kwa nini hamjatosheka bado kwa kula mwili
wangu? 23 Laiti, hayo maneno yangu yangekuwa yameandikwa chini! Laiti, hayo

yangekuwa yameandikwa katika kitabu! 24 Laiti, kwa kalamu ya chuma na risasi
hayo yangekuwa yamechorwa katika mwamba siku zote! 25 Lakini kama ilivyo
kwangu mimi, Mimi ninafahamu kwamba mkombozi wangu anaishi, na kwamba
hata mwisho atasimama katika nchi; 26 baada ya ngozi yangu, hivyo ndivyo, mwili
huu, unaharibiwa, ndipo katika mwili wangu mimi Nitamwona Mungu. 27 Mimi
nitamwona yeye kwa macho yangu mwenyewe-Mimi, na siyo mtu mwingine. Moyo
wangu hushindwa ndani yangu mimi. 28 Kama mnatasema, 'Kwa jinsi gani tutamtesa
yeye? Mzizi wa mahangaiko yake unakaa katika yeye; 29 ndipo uwe umeogopeshwa
kwa ule upanga, kwa sababu ghadhabu huleta hukumu ya upanga, hivyo kwamba
wewe uweze kutambua kuna hukumu.”

# 20

1 Ndipo Sofari, Mnaamathi alijibu na kusema, 2 “Mawazo yangu yananifanya mimi
nijibu kwa haraka kwa sababu ya mashaka yaliyomo ndani yangu mimi. 3 Mimi
ninasikia kukemewa ambako kunaniondolea heshima mimi, lakini roho kutoka
katika ufahamu wangu hunijibu mimi. 4 Je, unafahamu kwamba ukweli huu kutoka
enzi za kale, wakati Mungu alipomweka mwanadamu juu ya nchi: 5 ushindi wa
mtu mwovu ni mfupi, na furaha ya mtu asiyemcha Mungu hudumu kwa kitambo
tu? 6 Ingawa urefu wake yeye hufikia juu kwenye mbingu, na kichwa chake yeye
kufikia kwenye mawingu, 7 bado mtu huyo atapotea siku zote kama mavi yake yeye
mwenyewe; wale waliokuwa wamemuona yeye watasema, 'Yuko wapi yeye'? 8 Yeye
atapaa mbali kama ndoto na hataonekana; ndivyo ilivyo, yeye atakuwa amefukuzwa
mbali kama ono la 9 usiku. Jicho ambalo lilimuona yeye halitamuona yeye tena;
mahali pake hapatamuona yeye tena. 10 Watoto wake wataomba msamaha kwa
watu maskini, mikono yake itaweza kurudisha utajiri wake. 11 Mifupa yake imejaa
nguvu za ujanani, lakini zitalala naye chini katika mavumbi. 12 Japokuwa uovu ni
mtamu katika mdomo wake yeye, japokuwa yeye anauficha chini ya ulimi wake yeye,
13 japokuwa anaushikilia pale na hauruhusu kwenda lakini bado huushikilia katika
mdomo wake yeye - 14 chakula katika koromeo lake yeye hugeuka kuwa uchungu;
hugeuka kuwa sumu ya majoka ndani yake yeye. 15 Yeye humeza chini utajiri, lakini
yeye atautapika tena; Mungu atautoa nje kutoka katika tumbo lake yeye. 16 Yeye
atamumunya sumu ya majoka; ulimi wa nyoka mwenye sumu utamwua yeye. 17 Yeye
hatafurahia vijito vya maji, wingi wa asali na siagi. 18 Yeye atayarudisha matunda
ya kazi yake na hataweza kuyala; yeye hatafurahia utajiri alioupata kwa biashara
zake yeye. 19 Kwa kuwa yeye amewakandamiza na kuwasahau watu maskini; yeye
kwa uonevu, amezichukua mbali nyumba ambazo hakuzijenga yeye. 20 Kwa sababu
yeye mwenyewe hakujua utoshelevu wowote, yeye hataweza kuokoa kitu chochote
katika kile ambacho alijifurahisha. 21 Hakuna chochote kilichoachwa ambacho yeye
hakukimeza; kwa hiyo mafanikio yake yeye hayatakuwa ya kudumu. 22 katika
wingi wa utajiri wake yeye ataanguka katika mahangaiko; mkono wa kila mmoja
ambaye yuko katika umaskini utakuja kinyume chake yeye. 23 Wakati akiwa katika
kulijaza tumbo lake, Mungu atatupa hasira ya ghadhabu yake juu yake yeye; Mungu
ataunyeshea chini juu yake yeye wakati yeye anakula. 24 Ingawa mtu huyo atakimbia
kutoka katika silaha ya chuma, upinde wa shaba utampiga yeye. 25 Mshale utatoboa
kupitia mgongoni mwake na utatokezea; ni dhahiri, ncha inayong'ra itatokezea nje
kupitia ini lake yeye; watesi huja tena juu yake. 26 Giza lliilo kamilika limetunzwa kwa
akiba zake; moto usiopulizwa utamla yeye kwa haraka; utameza kile kilichoachwa
katika hema yake. 27 Mbingu zitauweka wazi uovu wake, na nchi itainuka juu
dhidi yake yeye kama shahidi. 28 Utajiri wa nyumba yake utatoweka; bidhaa zake

zitamwagika mbali siku ya ghadhabu ya Mungu. 29 Hii ndiyo sehemu ya mtu mwovu
kutoka kwa Mungu, urithi uliotunzwa akiba na Mungu kwa ajili yake yeye."

# 21

1 Kisha Ayubu akajibu na kusema, 2 "Sikilizeni hotuba yangu kwa makini, hii
na iwe faraja yenu. 3 Nimeteswa, lakini pia nitasema; nikisha kusema, endeleeni
kudhihaki. 4 Lakini kwangu mimi, malalamikio yangu ni kwa mtu? Kwa nini nisiwe
mwenye subira? 5 Nitazameni na mshangae, nanyi wekeni mkono wenu midomoni
mwenu. 6 Ninapoyafikiria mateso yangu, ninaumizwa, mwili wangu unaogopa. 7 Kwa
nini waovu wanaendelea kuishi, wanazeeka, na kuwa na uwezo katika madaraka?
8 Wazao wao wanathibitishwa mbele zao, na uzao wao unaimarika machoni pao.
9 Nyumba zao ziko salama mbali na hofu; wala fimbo ya Mungu haiko juu yao.
10 Dume lao la ng'ombe linazalisha; halishindwi kufanya hivyo; ng'ombe wao anazaa
na hafishi ndama wake akiwa mchanga. 11 Wanawapeleka wadogo wao kama kundi
la kondoo, na watoto wao hucheza. 12 Wanaimba kwa tari na vinubi na hufurahi kwa
muziki na zomari. 13 Wanatumia siku zao katika mafanikio, na wanashuka kuzimu
kwa utulivu. 14 Wanamwambia Mungu, 'Ondoka kwetu kwani hatutaki ufahamu
wowote juu ya njia zako. 15 Mwenye enzi ni nani, hata tumwabudu? Tutafaidika na
nini tukimwabudu? Tutapata faida gani ikiwa tutamwomba? 16 Tazama, je mafanikio
yao hayamo katika mikono yao wenyewe? Sina cha kufanya na ushauri wa waovu.
17 Mara ngapi taa za waovu huzimwa, au kwamba majanga huja juu yao? Mara
ngapi inatokea kwamba Mungu husambaza huzuni kwao kwa hasira? 18 Ni mara
ngapi inatokea kwamba wanakuwa kama mabua mbele ya upepo au kama makapi
yanayopeperushwa na dhoruba? 19 Mnasema, 'Mungu huweka hatia ya mtu kwa
watoto wake kuilipa.' Na alipe yeye mwenyewe, ili kwamba aweze kujua hatia
yake mwenyewe. 20 Acha macho yake yaone uangamivu wake mwenyewe, na acha
anywe gadhabu ya Mwenyezi. 21 Kwani anaangaliaje familia yake mbele yake idadi
ya miezi yake inapokwisha. 22 Je kuna mtu anaweza kumfundisha Mungu maarifa
kwa kuwa yeye huwaukumu hata walio juu? 23 Mtu mmoja ufa katika nguvu zake
kamili, akiwa na utulivu kabisa na kwa amani. 24 Mwili wake hauna uhitaji, na kiini
cha mifupa yake ina unyevu na afya njema. 25 Mtu mwingine ufa kwa uchungu
wa nafsi, bila kujifurahisha kwa jambo lolote jema. 26 Wanazikwa kaburini wote
kwa pamoja, funza wanawafunika wote. 27 Tazama, nayajua mawazo yenu, na
jinsi mnavyotaka kunikosesha. 28 Kwa kuwa mwasema, 'Iko wapi sasa nyumba ya
mwana wa mfalme? Liko wapi kao alipokaa mwovu?' 29 Je hamjawauliza wasafiri?
Hamfahamu wanavyoweza kusema, 30 kwamba mwovu anaepushwa na siku ya
shida, na kwamba anawekwa mbali na siku ya gadhabu? 31 Ni nani atakaye ituhumu
siku ya mwovu mbele yake? Ni nani atakayemwadhibu kwa alichokifanya? 32 Hata
hivyo atapelekwa kaburini; watu wataliona kaburi lake. 33 Udongo wa bondeni
utakuwa mtamu kwake; watu wote watamfuata, hata kuwe na watu wengi mbele
yake. 34 Ni jinsi gani basi mtanifariji bila kufikiri, kwa kuwa majibu yenu hayana
lolote ila uongo?"

# 22

1 Kisha Elifazi Mtemani akajibu na kusema, 2 Je mtu anaweza kumfaa Mungu "Je
mwenye hekima anaweza kufaa kwake. 3 Je inafurahisha kwa Mwenyezi ikiwa
u mwenye haki? Je ni faida yake ukiyafanya safi maisha yako? 4 Je ni kwa
sababu ya uchaji wako kwake hata akukemee na kukuadhibu? 5 Je si kwa sababu
ya wingi wa uovu wako? Je hakuna mwisho wa makosa yako? 6 Kwa maana
umechukua dhamana kutoka kwa ndugu yako bila sababu; umechukua mavazi ya

mtu na kumwacha uchi. 7 Haukuwapa wenye kiu maji ya kunywea; umewanyima
chakula wenye njaa 8 japokuwa wewe, mwenye uwezo, uliimiliki nchi, japokuwa
wewe, mwenye kuheshimiwa, uliishi ndani yake. 9 Umewaacha wajane waondoke
bila kitu; umewatesa yatima. 10 Kwa hiyo, mabaya yanakuzunguka, na hofu za
ghafla zinakusumbua. 11 Kuna giza, hata usione; gharika inakufunika. 12 Je Mungu
hayupo juu mbinguni? Anaangalia juu ya nyota, jinsi zilivyo juu! 13 Unasema,
'Mungu anajua nini? Je anaweza kuamua kupitia giza totoro? 14 Mawingu ni
kifuniko chake, hata asituone; anatembea anga la mbinguni.' 15 Je utayaishi maisha
ya zamani walioishi waovu - 16 walioondolewa kabla ya siku zao, ambao misingi
yao imeondolewa kama mto, 17 waliomwambia Mungu, 'Ondoka kwetu'; waliosema,
'Mwenyezi anaweza kututenda nini? 18 Hata hivyo bado alizijaza nyumba zao kwa
mema; mipango ya waovu iko mbali nami. 19 Wenye haki wanayaona yawapatayo
waovu na kufurahi; wasio na hatia wanawacheka kwa dhihaka. 20 Wanasema,
'Bila shaka walioinuka kinyume chetu wameondolewa; moto umeteketeza mali zao.'
21 Basi patana na Mungu na uwe na amani naye; kwa njia hiyo, mema yatakujia.
22 Nakusihi, pokea, maelekezo yake; uyatii maneno yake. 23 Ukimrudia Mwenyezi,
utajengwa, ukiacha kutenda uovu makaoni mwako. 24 Weka hazina zako mavumbini,
dhahabu ya Ofiri kati ya mawe ya vijito, 25 na Mwenyezi atakuwa hazina zako, fedha
ya thamani kwako. 26 Nawe utajifurahisha katika Mwenyezi; utamwangalia Mungu.
27 Utamwomba, naye atakusikiliza; utamtolea nadhiri. 28 Lakini pia utatamka lolote,
nawe utapewa; nuru itaangaza maishani mwako. 29 Mungu humshusha mwenye
kiburi, naye humwinua mnyenyekevu. 30 Atamwokoa asiye na hatia; utaokolewa
kupitia usafi wa mikono yako."

# 23

1 Kisha Ayubu akajibu na kusema, 2 "Hata leo malalamiko yangu ni machungu;
maumivu yangu ni mazito kuliko manung'uniko yangu. 3 Ee, ningejua niweza-
pokumwona! Ee, kwamba ningeweza kwenda alipo! 4 Ningeweka shitaka langu
mbele yake na kukijaza kinywa changu hoja. 5 Ningejua ambavyo angenijibu
na kufahamu ambavyo angesema juu yangu. 6 Je angehojiana nami katika ukuu
wa nguvu zake? Hapana, angenisikiliza. 7 Pale mwenye haki angehojiana nami.
Kwa njia hii ningeonekana bila hatia kwa mwamzi wangu. 8 Tazama, naelekea
mashariki, lakini hayupo pale, na upande wa magharibi, lakini siwezi kumwona.
9 Kaskazini, anapofanya kazi, lakini siwezi kumwona, na kusini, anapojificha hata
nisimwone. 10 Lakini anaijua njia ninayoichukua; atakapokuwa amenipima, nitatoka
kama dhahabu. 11 Mguu wangu umeunganishwa na hatua zake; nimezitunza njia
zake na sijageuka. 12 Sijaiacha amri ya midomo yake; nimeyatii maneno ya kinywa
chake. 13 Lakini yeye ni wa pekee, naniawezaye kumgeuza? Analolitaka, hulitenda.
14 Kwa maana hulitimiza agizo lake kinyume changu; anamipango mingi kwa ajili
yangu; ipo mingi kama hiyo. 15 Kwa hiyo, nimetishwa mbele zake; ninapofikiri
kumhusu, ninamwogopa. 16 Kwani Mungu ameudhoofisha moyo wangu; Mwenyezi
amenitisha. 17 Si kwa sababu nimeondolewa na giza, wala siyo kwamba giza nene
limeufunika uso wangu.

# 24

1 Kwa nini nyakati za kuwahukumu waovu hazikuwekwa na Mwenyezi? Kwa
nini siyo wale waliowaaminifu kwa Mungu huziona siku za hukumu zikija? 2 Kuna
waovu waondoao alama za mipaka; kuna waovu walichukua kundi kwa nguvu na
kulifanya lao. 3 Wanawadhurumu wanyonge punda wao; wanachukua ng'ombe wa
mjane kuwa dhamana. 4 Wanawaondoa wahitaji katika njia zao kwa lazima; masikini

wa dunia yote wanajificha kutoka kwao. 5 Tazama, masikini hawa huenda kufanya
kazi kama punda-mwitu mwituni, akitafuta chakula kwa uangalifu; pengine Araba
itawapatia chakula kwa ajili ya watoto wao. 6 Masikini huvuna katika mashamba
ya wengine usiku; wanakusanya zabibu kidogo kutokana na mapato ya waovu.
7 Wana lala bila kujifunika wakati wa usiku; hawana cha kujifunika wakati wa
baridi. 8 Wanalowanishwa na mvua ya milimani; wanalala pembeni mwa miamba
mikubwa kwani hawana makao. 9 Kuna waovu wanaowapokonya yatima katika
kifua cha mama zao, na waovu wawachukuao watoto kama dhamana kutoka kwa
masikini. 10 Lakini masikini wanatembea uchi; wajapokaa na njaa, wanabebea
wengine chakula. 11 Masikini wanazalisha vinono ndani ya nyumba za waovu;
wanakanyaga mashinikizo ya waovu, lakini wanakiu. 12 Watu wananung'unika
mjini; waliojeruhiwa wanaomboleza, lakini Mungu hasikilizi maombi yao. 13 Baadhi
ya waovu hawa wanaiasi nuru; hawafahamu njia zake, wala kukaa katika njia
zake. 14 Muaji huinuka na nuru; huuwa masikini na waitaji; ni kama mwizi
wakati wa usiku. 15 Pia, mzinifu hungoja wakati wa usiku; husema, 'Hakuna
anionaye.' Hujibadilisha. 16 Waovu huingia katika nyumba gizani, lakini hujifungia
wakati wa mchana; hawajari nuru. 17 Kwa kuwa asubuhi kwao wote ni kama
giza totoro; wanaamani na vitisho vya giza totoro. 18 Wanapotea polepole, lakini,
kama povu juu ya maji; shamba lao limelaaniwa; hakuna anayekwenda kufanya
kazi katika mashamba yao ya mizabibu. 19 Kiangazi na joto huondoa barafu;
ndivyo kuzimu pia kunavyowaaribu waliotenda dhambi. 20 Mama yake atamsahau;
polepole funza watamuuma; hatakumbukwa tena; kwa hiyo, waovu watavunjika
kama mti. 21 Mwovu anamrarua mgumba; hawatendi jema lolote kwa mjane. 22 Bado
Mungu huwaondoa wenye nguvu kwa nguvu zake; huinuka na kuwadhoofisha.
23 Mungu huwaacha wajione wako salama, na wanalifurahia hilo, lakini anayaangalia
maisha yao. 24 Watu hawa wanatukuzwa; bado, kitambo tu, watapotea; hakika,
watashushwa; watakusanywa kama wengine wote; wataondolewa kama sehemu ya
juu ya masikio ya nafaka. 25 Ikiwa sivyo, nani atanithibitisha kuwa mwongo; atakaye
fanya maneno yangu kuwa si kitu?”

## 25

1 Kisha Bilidadi Mshuhi akajibu na kusema, 2 “Utawala na hofu vipo naye; anaagiza
mahali pa juu pake mbinguni. 3 Je kuna idadi ya majeshi yake? Ni wapi pasipo
na nuru yake? 4 Jinsi gani basi mtu awe mwenye haki kama Mungu? Jinsi gani
aliyezaliwa na mwanamke awe safi, amekubaliwa naye? 5 Tazama, hata mwezi
kwake haungazii; nyota hazikosafi mbele zake. 6 Ni vipi mtu, aliyemdudu - mwana
wa mtu, aliye mdudu!”

## 26

1 Kisha Ayubu akajibu na kusema, 2 “Mmemsaidiaje aliyedhaifu! 3 Jinsi gani
mmemshauri asiye na hekima na kutamka maneno yenye maarifa kwake! 4 Kwa
msaada wa nani mmesema maneno haya? Ni roho ya nani iliyotoka ndani yenu?
5 Maiti inatetemeka chini ya maji, na vyote wilivyomo ndani yake. 6 Kuzimu kuko
wazi mbele ya Mungu; uharibifu hauna kizuizi dhidi yake. 7 Huitandaza kaskazi
juu ya nafasi wazi na kuining'iniza dunia hewani. 8 Huyafunga maji katika mawingu
yake mazito, lakini hayagawanyiki chini yake. 9 Huufunika uso wa mwezi na kueneza
mawingu yake juu yake. 10 Amechora ukingo wa duara juu ya maji kama mpaka kati
ya nuru na giza. 11 Nguzo za mbinguni zinatikisika na zimestushwa na kukemea
kwake. 12 Aliituliza bahari kwa uwezo wake; kwa ufahamu wake alimwaribu Rahab
13 Kwa pumzi yake, aliziondoa mbingu kwa dhorubu; mbingu ziliondolewa kwa

dhorubu; mkono wake ulimchoma nyoka anayekimbia. 14 Tazama, hizi si zaidi
ya madogo ya njia zake; Jinsi gani tunasikia akitunong'oneza! Ni nani awezaye
kufahamu uwezo wake.

## 27

1 Ayubu akaendelea kuoengea na kusema, 2 “Kama aishivyo Mungu, ameniondolea
haki yangu, Mwenyezi, aliyeyafanya machungu maisha yangu, 3 kadili uhai ungalimo
ndani yangu uzima wa Mungu upo puani mwangu. 4 Hakika midomo yangu
haitanena uovu, wala ulimi wangu kunena uongo. 5 Sitakiri kwamba mko sahihi;
hata nifapo sitakana uadilifu wangu. 6 Naishikilia haki yangu na sitaiacha; nafsi
yangu haitanisuta kadili ninavyoishi. 7 Adui yangu na awe kama mwovu; anayeinuka
kunyume changu na awe kama asiye haki. 8 Kwani tumaini la mwovu ni nini
Mungu anapomwondoa, Mungu anapochukua uhai wake? 9 Je Mungu atasikiliza kilio
chake tabu zinapompat? 10 Je atajifurahisha katika Mwenyezi na kumwita Mungu
nyakati zote 11 Nitawafundisha kuhusu uwezo wa Mungu; sitabatilisha mawazo ya
Mwenyezi. 12 Tazama, ninyi nyote mmeona; kwa nini basi mmeongea yasiyo na
maana. 13 Hii ndiyo hatima ya waovu mbele za Mungu, urithi wa mtesaji aupokeao
kutoka kwa Mwenyezi. 14 Ikiwa watoto wake wataongezeka, ni kwa upanga; uzao
wake utakuwa na njaa. 15 Wanaomsalia watauawa kwa tauni, na wajane wao
hawatawaombolezea. 16 Japokuwa waovu hurundika mali kama mavumbi, 17 na
kukusanya mavazi kama udongo, atakusanya mavazi, lakini mwenye haki atavaa,
na wasio na hatia watagawana mali. 18 Hujenga nyumba yake kama buibui,
kama kibanda cha muda afanyacho mlinzi. 19 Hulala kitandani akiwa tajiri, lakini
hataendelea hivyo; na afumbuapo macho, hana kitu. 20 Vitisho humpata kama maji,
dhoruba humwondoa usiku. 21 Upepo wa mashariki umwondoa, naye huondoka;
humwondoa mahali pake. 22 Humpiga bila kukoma; hujaribu kumnasua katika
uwezo wake. 23 Unampigia makofi kwa kejeli; humwondoa mahali pake.

## 28

1 Hakika kuna machimbo ya fedha, wanaposafisha dhahabu. 2 Chuma uchimbwa;
shaba uyeyushwa kutoka katika jiwe. 3 Mtu anaondoa giza na kutafuta, katika mpaka
wa mbali, mawe hayaonekani na giza totoro. 4 Huchimba shimo mbali na makazi ya
watu, mahali pasipopitwa na mtu. Huning'inia mbali na watu; uharakisha kwenda
na kurudi. 5 Kwa nchi, kizalishwapo chakula, inapinduliwa kama kwa moto. 6 Mawe
yake yana johari, na vumbi lake lina dhahabu. 7 Hata ndege mwindaji hapajui, wala
jicho la kipanga halijapaona. 8 Ndege mwenye majivuna hajawai kuiona njia hiyo,
wala simba mkali kupita pale. 9 Mtu huchimba mwamba mgumu; hupindua milima
katika vyanzo vyake. 10 Huweka njia katika miamba; macho yake pale kila kilicho
cha thamani. 11 Hufunga vyanzo hata wasiondoke; kilichofichika pale hukifunua.
12 Hekima itakuwa wapi? Mahali pa ufahamu ni wapi? 13 Mtu hafahamu thamani
yake; wala haipatikani katika nchi ya walio hai. 14 Vilindi vya maji chini ya nchi
husema, 'Haiko kwangu'; bahari husema, 'Haipo pamoja nami.' 15 Hainunuliwi kwa
dhahabu; wala hailinganishwi na fedha. 16 Haiwezi kuthamanishwa na dhahabu ya
Ofiri, kwa jiwe jeusi la thamani au johari. 17 Dhahabu na fuwele hailingani nayo kwa
thamani; wala haiwezi kubadilishwa kwa vito vya dhahabu safi. 18 Hailinganishwi na
marijani wala yaspi; hakika, thamani ya hekima inapita madini ya rubi. 19 Topazi ya
Ethiopia hailinganishwi nayo; wala kuthamanishwa kwa dhahabu safi. 20 Je hekima
inatoka wapi? Mahali pa ufahamu ni wapi? 21 Hekima imejificha mbali na macho
ya viumbe wote na ndege wa angani. 22 Mauti na uharibifu husema, 'Tumesikia tu
tetesi kwa masikio yetu.' 23 Mungu hufahamu njia ya kuipata; anapafahamu ilipo.

24 Kwani uona miisho yote ya dunia na huona chini ya mbingu zote. 25 Hapo kale,
alifanya nguvu za upepo na kuyagawanya maji kwa kipimo. 26 Aliiwekea mvua tamko
na njia ya radi na munguromo. 27 Kisha akaiona hekima na kuitangaza; aliianzisha,
bila shaka, na kuipima. 28 Aliwambia watu, 'Tazameni, kumcha Bwana - ni hekima;
kuacha uovu ni ufahamu.”

# 29

1 Ayubu akaendelea na kusema, 2 Ee, ningekuwa kama nilivyokuwa miezi
iliyopita wakati Mungu aliponiagalia, 3 taa yake ilipowaka kichwani pangu, na pale
nilipotembea gizani kwa nuru yake. 4 Ee, kwamba ningekuwa kama nilivyokuwa
katika siku za ujana wangu uhusiano wangu na Mungu ulivyokuwa mzuri, 5 wakati
Mwenyezi alipokuwa pamoja nami, na wanangu walipokuwa karibu nami, 6 wakati
maisha yangu yalipokuwa yamejawa na utele, na mwamba uliponichuruzishia
chemichemi za mafuta. 7 Nilipokwenda langoni mwa mji, nilipokaa katika eneo la
mji, 8 vijana waliniona na walikaa mbali kwa kuniheshimu, na wazee waliinuka
na kusimama kwa ajili yangu. 9 Wana wa mfalme waliacha kuongea nilipofika;
wangeweka mkono wao katika vinywa vyao. 10 Sauti za waheshimiwa zililazimishwa,
na ndimi zao hazikuweza kuongea vinywani mwao. 11 Kwani baada ya kunisikia,
wangenibariki; waliponiona, wangeniona na kuniheshimu 12 kwa maana nilikuwa
nikiwasaidia masikini waliokuwa wakiteseka, na yatima, asiye na msaada. 13 Baraka
zao waliokuwa karibu kuangamia zilinipata; niliufanya moyo wa mjane kuimba
kwa furaha. 14 Nilijivika utakatifu, nao ulinifunika; haki yangu ilikuwa kama
kanzu na kilemba. 15 Niliwasaidia vipofu; niliwasaidia walemavu. 16 Niliwasaidia
wahitaji; niliwasaidia hata wasionijua. 17 Nilimnyamazisha mwovu; nilimpokonya
manusura kutoka katika meno yake. 18 Kisha nilisema nitakufa mahali salama;
nitazizidisha siku zangu kama mchanga. 19 Mizizi yangu imeenea majini, na
umande kukaa usiku wote katika matawi yangu. 20 Heshima yangu ni mpya
daima, na nguvu za upinde wangu zipo katika mkono wangu kila wakati. 21 Watu
walinisikiliza; walinisubiri; walisikiliza ushauri wangu. 22 Nilipo maliza kuongea
hawakunena tena, maneno yangu yaliwatia nguvu kama mvua. 23 Waliningoja kama
kungoja mvua; waliyathamini maneno yangu, kama walivyotamani mvua iliyokawia.
24 Niliwafurahia bila wao kutarajia; hawakukataa uzuri wa uso wangu. 25 Nilikuwa
kama mfalme wao na kuwachagulia cha kufanya; nilikuwa kama mfalme katika jeshi
lake, kama awafarijiye waombolezaji mazishini.

# 30

1 Sasa vijana wananidhihaki - vijana ambao baba zao wasingeweza hata kuwahudu-
mia mbwa wa kundi langu. 2 Kwa kweli, nguvu za mikono ya baba zao,
zingenisaidia nini - watu ambao hawakuwa na nguvu wakati wa kukua kwao?
3 Walidhoofishwa na umasikini na njaa; walisaga nchi kavu mafichoni. 4 Walichuma
mche chumvi na majani ya vichaka; mizizi ya mti wa ufagio ilikuwa ndiyo chakula
chao. 5 Waliondolewa miongoni mwa watu waliopiga kelele nyuma yao kama
ambavyo mtu angempigia kelele mwizi. 6 Hivyo walipaswa kuishi katika mabonde
ya mto, katika mashimo ya ardhi na miamba. 7 Walilia kwa uchungu porini
kama punda; chini ya vichaka walikutana. 8 Walikuwa uzao wa wapumbavu,
hakika, wa watu wasiofaa; waliondolewa duniani kama waarifu. 9 Lakini sasa,
nimekua sababu ya wimbo wa dhihaka kwa wana wao; hakika, nimekuwa mzaa
kwao. 10 Wananichukia na kusimama mbali nami; hawaachi kunitemea usoni.
11 Kwa maana Mungu ameondoa kamba katika upinde wangu na amenipiga, na
hivyo watu hawa wanashindwa kujizuia mbele yangu. 12 Kundi la vijana wabaya

wanashambulia nguvu zangu; wananiondolea mbali na kukusanya kinyume changu
rundo la kuhusuru. 13 Wanaharibu maisha yangu; wanapeleka mbele maangamizi
yangu, watu wasio na wakuwazuia. 14 Wanakuja kinyume changu kama jeshi katika
tundu pana katika ukuta wa mji; katikati ya maangamizi wanajizungusha juu yangu.
15 Hofu zimeniandama; heshima yangu imeondolewa mbali nami kama kwa upepo;
mafanikio yangu yameondolewa kama wingu. 16 Sasa uhai wangu umeondolewa
ndani yangu; siku nyingi za maumivu zimenipita. 17 Mifupa inauma ndani yangu
wakati wa usiku; maumivu yanayonisaga hayaishi. 18 Nguvu kuu ya Mungu
imeshika mavazi yangu; yananizunguka kama kala ya vazi langu. 19 Amenitupa
matopeni; nimekuwa kama vumbi na majivu. 20 Nakulilia wewe, Mungu, lakini
haunijibu; ninasimama, nawe unaniangalia tu. 21 Umegeuka na kuwa mkali kwangu;
kwa nguvu za mkono wako umenitesa. 22 Unaniinua katika upepo na kuufanya
unikokote; unanirusha huku na kule katika dhoruba. 23 Kwa maana najua ya kwamba
utanipeleka mautini, nyumba ya hatima kwa viumbe vyote. 24 Lakini, je hakuna
ainuaye mkono wake kuomba msaada aangukapo? Je hakuna aombaye msaada
akiwa tabuni? 25 Je sikulia kwa ajili yake aliyekuwa tabuni? Je sijahuzunika kwa ajili
ya mwitaji? 26 Nilipotazamia mema, ndipo yalipokuja mabaya; niliposubiri nuru,
giza lilikuja badala yake. 27 Moyo wangu umetaabika na hautulii; siku za mateso
zimenipata. 28 Nimekuwa na ngozi nyeusi lakini si kwa sababu ya jua; nasimama
katika kusanyiko na kulilia msaada. 29 Nimekuwa ndugu kwa mbwea, mshirika wa
mbuni. 30 Ngozi yangu imekuwa nyeusi na inapukutika; mifupa yangu imeunguzwa
na joto. 31 Kwa hiyo kinubi changu kimefunguliwa kwa nyimbo za maombolezo,
zomari yangu kwa kuimba kwao waombolezao.

# 31

1 Nimefanya patano na macho yangu; ni kwa namna gani tena napaswa kumtazama
mwanamwali kwa tamaa? 2 Ni sehemu gani kutoka kwa Mungu juu, na urithi gani
kutoka kwake mwenye nguvu aliye juu? 3 Nilikuwa nafikiri kwamba majanga ni
kwa watu wasio na haki, na misiba ni kwa ajili ya watu watendao mabaya. 4 Je
Mungu hazioni njia zangu na kuzihesabu hatua zangu zote? 5 Kama nimetembea
katika udanganyifu, kama mguu wangu umeharakisha katika uongo, 6 na nipimwe
katika vipimo vilivyo sawa ili kwamba Mungu aujue uadilifu wangu. 7 Kama
hatua zangu zimegeuka kutoka katika njia sahihi, kama moyo wangu umetembea
kwa kufuata macho yangu, na kama doa lolote la uchafu limeng'ang'ania katika
mikono yangu, 8 na kisha mimi nipande na mtu mwingine na ale; mavuno na
yang'olewe katika shamba langu. 9 Na kama moyo wangu umevutiwa na mwanamke
mwingine, ikiwa nimelala na mke wa jirani yangu katika hali ya kusubiria katika
mlango wake, 10 na ndipo mke wangu na asage nafaka kwa mwanaume mwingine,
na wanaume wengine na walale naye. 11 Na kwa hilo litakuwa ni kosa kubwa;
kwa kweli, utakuwa ni uovu wa kuadhibiwa na waamuzi. 12 Kwa kuwa ni moto
ambao unateketeza kila kitu kwa uharibifu, na kwamba utaunguza mavuno yangu
yote. 13 Ikiwa nilikataa ombi la haki kutoka kwa watumishi wangu wa kiume na
wa kike wakati walipohojiana nami, 14 kisha nini basi ningefanya wakati Mungu
anapoinuka ili kunishitaki mimi? Atakapokuja kunihukumu, nitamjibuje? 15 Je
yeye aliyenifanya mimi tumboni hakuwafanya wao pia? Je yeye si yeye yule
aliyetuumba sisi wote katika tumbo? 16 kama nimewanyima watu masikini matakwa
yao, au kama nimesababisha macho ya wajane yafifie kwa kulia, 17 au ikiwa
kama nimekula kipande changu na sijawaruhusu wale wasio na baba kukila pia
- 18 kwasababu tangu ujana wangu yatima walikua pamoja nami kama kuwa na
baba, nami nimemwongoza mama yake, mjane, tangu katika tumbo la mama yangu

mwenyewe. [19] ikiwa nimemwona yeyote akiangamia kwa kwa kukosa mavazi, au
kama nimemwona mtu mhitaji akiwa hana nguo; [20] ikiwa moyo wake haujanibariki
kwasababu amekuwa hajatiwa joto na sufu ya kondoo zangu, [21] ikiwa nimeinua juu
mkono wangu kinyume na watu wasio na baba kwa kuwa niliona msaada wangu
katika lango la mji, na kisha kuleta mashitaka dhidi yangu. [22] Ndipo bega langu
na lianguake kutoka katika sehemu yake, na mkono wangu uvunjike katika kiungo
chake. [23] Kwa kuwa niliogopa uharibifu kutoka kwa Mungu; kwasababu ya mawazo
ya ukuu wake, nisingeweza kufanya mambo hayo. [24] Kama ningeifanya dhahabu
kuwa tumaini langu, na kama ningesema kwa dhahabu safi, 'wewe unanifanya kuwa
na tumaini'; [25] na kama nimefurahi kwasababu ya utajiri wangu ulikuwa mkubwa,
kwa kuwa mkono wangu umepata mali nyingi, na kisha kuleta mashitaka dhidi
yangu! [26] Ikiwa nimeliona jua lilipowaka, au mwezi ukitembea katika mng'ao wake,
[27] na kama moyo wangu umevutwa kwa siri, ili kwamba mdomo wangu umeubusu
mkono wangu katika ibada yao - [28] hili nalo pia lingekuwa ni ubaya wa kuadhibiwa na
waamuzi, kwa kuwa ningekuwa nimemkana Mungu aliyejuu. [29] Ikiwa nimefurahia
uharibifu wa yeyote ambaye ananichukia mimi, au kuwapa hongera wakati majanga
yanapowapata, ndipo ulete mashitaka dhidi yangu! [30] Kwa kweli sijauruhusu hata
mdomo wangu kutenda dhambi kwa kuuomba uhai wake kwa laana. [31] Ikiwa watu
wa hema yangu hawajasema,' Nani aweza kumpata mtu ambaye hayashibishwa
na chakula cha Ayubu? [32] (hata mgeni hajawahi kukaa katika pembe ya mji, kwa
kuwa siku zote nimefungua milango yangu kwa ajili ya wasafiri), na kama haiko
hivyo, ndipo mlete mashitaka kinyume nami! [33] Ikiwa, kama binadamu nimezificha
dhambi zangu kwa kuficha hatia ndani ya kanzu yangu - [34] kwa kuwa niliogopa
kusanyiko kubwa, kwasababu ya matwezo ya familia yaliniogopesha, hivyo basi
nilinyamaza kimya na sikuweza kwenda nje, basi nileteni mashitaka dhidi yangu!
[35] Ee, kama nilikuwa na mtu wa kunisikiliza! Ona, hii ni saini yangu; na Mwenye
nguvu na anijibu! Ikiwa nilikuwa na shitaka rasmi ambalo adui yangu ameliandika!
[36] Hakika ningelibeba hadharani juu ya bega langu; ningeliweka juu kama taji.
[37] Ningemweleza hesabu ya hatua zangu; na kama mwana wa mfalme mwenye
kujiamini ningepanda kwenda kwake. [38] Kama nchi yangu ingelia dhidi yangu, na
matuta yake yaomboleza pamoja, [39] ikiwa nimekula mavuno yake bila kulipia au
kama nimesababisha wamiliki wake kupoteza maisha yao, [40] ndipo miiba na iote
badala ya ngano na magugu badala ya shayiri.” Maneno ya Ayubu yamemalizika.

# 32

[1] Hivyo hawa watu watatu walikoma kumjibu Ayubu kwasababu alikuwa ni
mwenye haki katika macho yake mwenyewe. [2] Ndipo iliwaka hasira ya Elihu
mwana wa Barakeli Mbuzi, wa familia ya Ramu, iliwaka dhidi ya Ayubu kwa
kuwa alijihesabia haki mwenyewe kuliko Mungu. [3] Hasira ya Elihu iliwaka pia
kinyume cha marafiki zake watatu kwasababu hawakupata jibu kwa ajili ya Ayubu,
na bado walimhukumu Ayubu. [4] Sasa Elihu alikuwa amemsubiri Ayubu ili aweze
kuzungumza naye kwa kuwa watu wengine walikuwa wakubwa kuliko yeye. [5] Hata
hivyo, wakati Elihu alipoona ya kuwa hapakuwa na jibu katika midomo ya watu
hawa watatu, hasira yake iliwaka. [6] Ndipo Elihu mwana wa Barakeli Mbuzi alinena
na kusema, “Mimi ni mdogo, na ninyi ni wazee. Hii ndio sababu nilijizuia na
sikuthubutu kuzungumza mawazo yangu mwenyewe. [7] Nilisema, “Urefu wa siku
utazungumza; na wingi wa miaka utatufundisha hekima. [8] Lakini kuna roho ndani
ya mtu; pumzi ya Mwenye nguvu humpa yeye ufahamu. [9] Si tu watu wakubwa
ndio wenye hekima, wala watu wazee pekee ambao hufahamu haki. [10] Hivyo basi
nakwambia wewe, “Nisikilizeni mimi; Nitakwambia pia uelewa wangu.' [11] Tazama,

niliyasubiria maneno yenu; nilisikiliza hoja zenu wakati mlipokuwa mnafikiri juu
ya kile cha kusema. [12] Hakika, niliwajali sana ninyi, lakini, tazama, hakuna hata
mmoja wenu aliyeweza kumshawishi Ayubu wala ambaye aliweza kumjibu maneno
yake. [13] Iweni waangalifu msije mkasema, 'Tumepata hekima!' Mungu atakuwa
amemshinda Ayubu; mtu wa kawaida hawezi akafanya hivyo. [14] Kwa kuwa Ayubu
hajasema mojamoja maneno yake juu yangu, basi sitamjibu kwa maneno yenu.
[15] Hawa watu watatu wamep igwa bumbuwazi; hawawezi kuendelea kumjibu Ayubu;
hawana neno zaidi la kusema. [16] Je ninapaswa kusubiria kwasababu hawazungumzi,
kwa kuwa wamesimama pale kimya na wala hawajibu zaidi? [17] La, nitajibu pia
upande wangu; Nitawaambia pia ufahamu wangu. [18] Kwa kuwa nimejawa na
maneno mengi, roho ndani yangu inanisukuma. [19] Tazama, kifua changu ni kama
divai yenye chachu ambayo haina tundu; kama viriba vipya, kiko tayari kupasuka.
[20] Nitazungumza ili kwamba niweze kuburudishwa; nitafungua kimya changu na
kusema. [21] Sitaonesha upendeleo; wala sitatoa sifa za majina kwa mtu yeyote. [22] Kwa
kuwa sijui namna ya kutoa sifa; kama nitafanya hivyo, Muumba wangu atanikatilia
mimi mbali.

# 33

[1] Kwahiyo sasa, nakuomba wewe, Ayubu, usikilize hotuba yangu; sikiliza maneno
yangu yote. [2] Tazama sasa, nimeufumbua mdomo wangu; ulimi wangu umesema
maneno ndani ya mdomo wangu. [3] Maneno yangu yatasema uadilifu wa moyo
wangu; yatasema kwa unyofu yale ambayo mdomo wangu unayajua. [4] Roho ya
Mungu imeniumba; pumzi ya Mwenye nguvu imenipatia uhai. [5] Kama unaweza,
nijibu; weka maneno yako katika mpangilio mbele yangu na kisha usimame.
[6] Tazama, niko kama wewe ulivyo mbele za Mungu; nimeumbwa pia kutoka katika
udongo. [7] Ona, tishio langu halitakufanya wewe uogope; wala mzigo wangu
hautakuwa mzito kwako. [8] Umesema kwa hakika katika masikio yangu; nimeisikia
sauti ya maneno yakeo yakisema, [9] 'Mimi ni safi na bila hila; sina hatia, na hakuna
dhambi ndani yangu. [10] Tazama, Mungu huona nafasi za kunishambulia mimi;
huniangalia mimi kama adui yake. [11] Huweka miguu yangu akiba; naye huangalia
njia zangu zote.' [12] Tazama, katika hili hauko sawa, nitakujibu, kwa kuwa Mungu
ni mkuu kuliko mtu. [13] Kwanini unashindana naye? Huwa hahesabu matendo
yake yoyote. [14] Kwa kuwa Mungu huzungumza mara moja, naam, mara mbili,
ingawa mwanadamu hawezi kutambua. [15] Katika ndoto, katika maono ya usiku,
wakati usingizi mzito unapowapata watu, katika usingizi kitandani - [16] basi Mungu
hufungua masikio ya watu, na kuwatisha kwa vitisho, [17] kwa kusudi la kumvuta mtu
atoke katika makusudio yake maovu, na kuyaweka majivuno mbali naye. [18] Mungu
huyaokoa maisha ya mwanadamu kutoka katika shimo, na uhai wake dhidi ya
kifo. [19] Mtu huadhidibiwa pia na maumivu kitandani mwake, na maumivu makali
yanayodumu katika mifupa yake, [20] ili kwamba maisha yake yachukie chakula,
na roho yake ichukie vyakula vizuri. [21] Nyama yake imeharibiwa ili kwamba
usionekane; mifupa yake, mara moja isionekane, sasa basi ng'ang'ania. [22] Hakika,
roho yake inasogea shimoni, na uhai wake unasogea kwa wale wanaotaka kuuharibu.
[23] Lakini kama kuna malaika anayeweza kuwa mpatanishi kwa ajili yake, mpatanishi
mmoja miongoni mwa maelfu ya malaika, kumwonesha kile kilicho cha haki ili
atende haki, [24] na kama malaika ni mpole kwake na kumwambia Mungu, 'Mwokoe
mtu huyu ili asishuke chini shimoni; nimepata fidia kwa ajili yake,' [25] kisha mwili
wake utakuwa mororo kuliko mwili wa mtoto, atazirudia siku za nguvu za ujana
wake. [26] Atamwomba Mungu, na Mungu atakuwa mwema kwake, ili kwamba auone
uso wa Mungu akiwa mwenye furaha. Mungu atampa mtu ushindi wake. [27] Ndipo

mtu huyo ataimba mbele ya watu wengine na kusema, 'Nilitenda dhambi na kuasi kile
kilichokuwa cha haki, lakini dhambi yangu haikuadhibiwa. 28 Mungu ameiokoa roho
yangu isiende chini shimoni; maisha yangu yataendelea kuuona mwanga.' 29 Tazama,
Mungu hufanya mambo haya yote pamoja na mwanadamu, mara mbili, naam, hata
mara tatu, 30 kuirudisha roho yake kutoka shimoni, ili kwamba aweze kumlikwa
na mwanga wa maisha. 31 Ayubu, zingatia na unisikilize mimi; nyamaza nami
nitasema. 32 Ikiwa una kitu cha kusema, na unijibu; sema, maana nataka kuhakikisha
kwamba wewe uko katika haki. 33 Kama sivyo, basi nisikilize, ubaki kimya, nami
nitakufundisha wewe hekima."

# 34

1 Zaidi ya hayo, Elihu aliendelea kusema: 2 "Sikilizeni maneno yangu, ninyi watu
wenye hekima; nisikieni, ninyi mlio na maarifa. 3 Kwa kuwa sikio huyajaribu maneno
kama ambavyo kaakaa huonja chakula. 4 Na tujichagulie sisi wenyewe yale yenye
adili: na tujigundulie miongoni mwetu yale yaliyo mazuri. 5 Kwa kuwa Ayubu
amesema, 'mimi ni mwenye haki, lakini Mungu ameondoa haki zangu. 6 Pamoja
na haki zangu, ninaangaliwa kama mwongo. Kidonda changu hakiponyeki, ingawa
mimi sina dhambi.' 7 Ni mtu gani aliye kama Ayubu ambaye hunywa dharau
kama maji, 8 ambaye huzunguka katika ushirika wa watu ambao ni waovu, na
ambaye hutembea pamoja na watu waovu? 9 Kwa kuwa anasema, ' Hakuna faida
kwa mtu kujifurahisha kwa kufanya mambo ambayo Mungu anayataka.' 10 Basi
nisikilizeni mimi, enyi watu wenye ufahamu: na iwe mbali na Mungu kwamba
atatenda uovu; 11 na iwe mbali na Mwenye enzi kwamba atatenda dhambi. Kwa kuwa
humlipa mtu kutokana na kazi yake; na humfanya mtu apate thawabu za njia zake
mwenyewe. 12 Kwa hakika, Mungu hatendi uovu, wala Mwenye nguvu hajaIpotosha
haki. 13 Ni nani aliyemweka kuwa mtawala wa dunia? Ni nani aliyeiweka dunia
yote chini yake? 14 Ikiwa aliweka makusudio yake juu yake mwenyewe, na kama
amejikusanyia mwenyewe nafsi yake na pumzi yake, 15 basi miili yote itateketea
pamoja; mwanadamu angerudi mavumbini tena. 16 Kama sasa mna ufahamu,
sikilizeni haya; sikilizeni sauti ya maneno yangu. 17 Je yeye anayeichukia haki aweza
kutawala? Je mtamhukumu Mungu kuwa ni mwenye makosa, ambaye ni mwenye
haki na mwenye nguvu? 18 Mungu ambaye humwambia mfalme, ' Wewe ni mbaya;
au huwaambia wenye kuheshimiwa, 'Ninyi ni waovu'? 19 Mungu ambaye haoneshi
upendeleo kwa viongozi na ambaye hawakubali zaidi watu matajiri kuliko masikini,
kwa kuwa wote ni kazi ya mikono yake. 20 Watakufa kwa muda mfupi; wakati wa
usiku watu watatikiswa na watapita; watu wenye nguvu watatwaliwa mbali, lakini
si kwa mikono ya wanadamu. 21 Kwa kuwa macho ya Mungu yako juu ya njia za
mtu; anaziona hatua zake zote. 22 Hakuna giza, wala hakuna weusi mzito ambao
watenda mabaya wanaweza kujificha wao wenyewe. 23 Kwa kuwa Mungu hahitaji
kumchunguza mtu zaidi; wala hakuna haja kwa mtu yeyote kwenda mbele zake
kwa hukumu. 24 Huwavunja vipande vipande watu wenye nguvu kwa ajili ya njia
zao ambazo hazihitaji uchunguzi zaidi; huwaweka watu wengine katika nafasi zao.
25 Kwa namna hii ana maarifa juu ya matendo yao; huwatupa watu hawa wakati wa
usiku; nao wameangamizwa. 26 Huwaua kwa matendo yao mabaya kama wakosaji
dhahiri mbele za watu wengine 27 kwasababu wamegeuka na kuacha kumfuata yeye
na wamekataa kuzisadiki njia zake zozote. 28 Na kwa namna hii, wamekifanya kilio
cha watu masikini kimfikie; amekisikia kilio cha watu walioteswa. 29 Na wakati
akaapo kimya, nani aweza kumhukumu kuwa mkosaji? Kama akiuficha uso wake,
ni nani awezaye kumjua? Anatawala sawa sawa juu ya taifa na mtu pia, 30 ili
kwamba watu wasiomjua Mungu wasije wakatawala, ili kwamba asiwepo mtu wa

kuwanasa watu. 31 Fikiria mtu akimwambia Mungu, ' Mimi ni mwenye hatia kabisa,
lakini sitatenda dhambi tena; 32 nifunze kile ambacho siwezi kukiona; nimetenda
dhambi, lakini sitafanya tena.' 33 Je unadhani kwamba Mungu ataiadhibu dhambi
ya mtu huyo, kwa kuwa unayachukia yale ambayo Mungu huyatenda? Ni lazima
uchague, siyo mimi. Basi sema yale ambayo unayajua. 34 Watu wenye ufahamu
wataniambia, kwa kweli, kila mtu mwenye hekima ambaye hunisikia atasema,
35 Ayubu anazungumza bila maarifa; maneno yake hayana hekima.' 36 Kama Ayubu
alijaribiwa kwa kitu kidogo kabisa katika kesi yake kwasababu ya kuongea kwake
kama watu waovu. 37 Kwa kuwa anaongeza uasi juu ya dhambi yake; anapiga makofi
ya dharau kati yetu; anaweka maneno kinyume na Mungu."

# 35

1 Aidha, Elihu aliendelea kusema, 2 "Je unadhani hii ni sawa unaposema, 'Haki
yangu mbele ya Mungu? 3 Kwa kuwa unauliza, 'Inafaa nini kwangu' na 'Ingekuwa
nzuri kwangu kama ningekuwa nimetenda dhambi?' 4 Nitakujibu, wewe pamoja na
marafiki zako. 5 Tazama juu angani, na ulione; angalia anga, ambalo liko juu sana
kuliko wewe. 6 Kama umetenda dhambi, ni madhara gani huwa unayafanya kwa
Mungu? Ikiwa makosa yako yameongezeka zaidi, je huwa unafanya nini kwake?
7 Kama wewe ni mwenye haki, unaweza kumpa nini? Je atapokea nini mkononi
mwako? 8 Uovu wako waweza kuwaumiza mtu, kama ulivyo wewe ni mtu, na haki
yako yaweza kumnufaisha mwana mwingine wa mtu. 9 Watu wanalia kwasababu
ya matendo mengi ya unyanyasaji; wanaomba msaada katika mikono ya watu
wenye nguvu. 10 Lakini hakuna hata mmoja asemaye, ' Mungu Muumba wangu
yuko wapi, ambaye hutoa nyimbo wakati wa usiku, 11 ambaye hutufundisha sisi
zaidi anavyowafundisha wanyama wa dunia, na ambaye hutufanya sisi kuwa wenye
hekima kuliko ndege wa angani? 12 Huko wanalia, lakini Mungu hawajibu kwasababu
ya kibriu ya watu waovu. 13 Kwa hakika Mungu hatasikia kilio cha kipumbavu;
Mwenye nguvu wala hatajali. 14 Ni kwa namna gani atakujibu ikiwa unasema
haumwoni, na ya kwamba hoja yako iko mbele yake, na ya kuwa unamngojea yeye!
15 Ni kwa jinsi gani atakujibu kama unasema kwamba hamwadhibu yeyote kwa
hasira, na ya kwamba hajishughulishi na kiburi cha watu. 16 Basi Ayubu hufumbua
kinywa chake tu ili kusema upumbavu; huongeza maneno bila maarifa."

# 36

1 Elihu aliendelea na kusema, 2 "Niruhusu niseme kidogo zaidi, nami nitakuonesha
baadhi ya mambo kwasababu nina maneno machache ya kusema kwa ajili ya
Mungu. 3 Nitapata maarifa yangu kutoka mbali; nitatambua kwamba haki ni ya
Muumba wangu. 4 Kwa kweli, maneno yangu hayatakuwa ya uongo; mtu fulani
aliyekomaa katika maarifa yu pamoja nawe. 5 Angalia, Mungu ni mwenye nguvu,
na hamdharau mtu yeyote; yeye ni mwenye nguvu katika uweza wa ufahamu.
6 Yeye huwa hayahifadhi maisha ya watu waovu bali badala yake hufanya yaliyo
ya haki kwa wale wanaoteseka. 7 Haondoi macho yake kwa wenye haki bali
badala yake huwaweka juu ya viti vya enzi kama wafalme milele, nao wameinuliwa
juu. 8 Ikiwa wamefungwa minyororo na kunaswa katika kamba za mateso, 9 kisha
huwafunulia kile walichokifanya, na maovu yao na kiburi chao. 10 Hufungua pia
masikio yao kwa ajili ya agizo lake, na huwaamuru wageuke kutoka katika uovu.
11 Ikiwa watamsikiliza na kumwabudu yeye, wataishi katika mafanikio katika siku
zao, na miaka yao katika hali ya kuridhika. 12 Hata hivyo, kama hawatasikiliza,
wataangamia kwa upanga; watakufa kwasababu hawana maarifa. 13 Na wale
wasiomjua Mungu hutunza hasiria zao katika mioyo; hawaombi msaada hata wakati

ambapo Mungu huwafunga. 14 Hawa hufa katika ujana wao; na maisha yao
hukoma kati ya makahaba. 15 Mungu huwainua watu walioonewa kwa njia ya
mateso yao; hufungua masikio yao kwa njia ya uonevu wao. 16 Kwa hakika, yeye
angependa kuwatoa ninyi katika mateso na kuwaweka katika sehemu pana ambapo
hakuna masumbufu na mahali ambapo meza yenu ingewekwa ikiwa na chakula
kilichojaa mafuta. 17 Lakini wewe umejaa hukumu juu ya watu waovu; hukumu
na haki umeziachilia. 18 Usiuache utajiri ukuvute katika udanganyifu; na sehemu
kubwa ya rushwa isikugeuze upande kutoka katika haki. 19 Je utajiri wako waweza
kukunufaisha, ili kwamba usiwe katika taabu, au nguvu zako zote za uwezo zaweza
kukusaidia? 20 Usiutamani usiku ili utende dhambi dhidi ya wengine wakati ambapo
mataifa hukatiliwa mbali katika nafasi zao. 21 Uwe mwangalifu ili kwamba usigeukie
dhambi kwasababu unajaribiwa kwa mateso ili kwamba ukae mbali na dhambi.
22 Angalia, Mungu ameinuliwa katika nguvu zake; ni nani aliye mwalimu kama
yeye? 23 Ni nani alishamwalekeza njia yake? Nani anayeweza kumwambia, 'Wewe
umetenda mambo yasiyo ya haki?' 24 Kumbuka kuyasifu matendo yake, ambayo watu
wameyaimba. 25 Watu wote wameshayatazama hayo matendo, lakini wanayaona tu
matendo hayo kwa mbali sana. 26 Tazama, Mungu ni mkuu, lakini sisi hatumfahamu
yeye vizuri; hesabu ya miaka yake haihesabiki. 27 Kwa kuwa yeye huvuta matone
ya maji ili kuyachuja kama mvua katka mvuke wake, 28 ambayo mawingu yake
huyamwaga chini na kuyandondosha kwa wingi kwa mwanadamu. 29 Hakika, kuna
hata mmoja awezaye kuelewa kwa undani kusambaa kwa mawingu na radi kutoka
katika nyumba yake? 30 Angalia, hueneza mwanga wake kumzunguka na kufunika
mizizi ya bahari. 31 Kwa namna hii huyahukumu mataifa na kuwapa chakula kwa
wingi. 32 Yeye huuijaza mikono yake kwa mwanga mpaka pale anapouamuru kupiga
shabaha yake. 33 Na muungurumo wake huonya kwa dhoruba, wanyama wanaweza
kusikia kuja kwake.

# 37

1 Hakika, moyo wangu hutetemeka kwa hili; umeondolewa kutoka katika sehemu
yake. 2 Sikia, Ee, Sikia kelele za sauti yake, sauti inayotoka katika mdomo wake.
3 Huiagiza sauti chini ya mbingu yote, na huutuma mwanga wake katika mipaka ya
dunia. 4 Sauti huunguruma baada yake; yeye huunguruma kwa sauti ya ukuu wake;
hauzuii mshindo wa mwanga wakati sauti yake inaposikika. 5 Mungu huunguruma
kwa sauti yake kwa namna ya ajabu; yeye hufanya mambo makubwa ambayo sisi
hatuwezi kuyafahamu. 6 Kwa kuwa huiambia theluji, 'Angukeni juu ya dunia'; hali
kadhalika kwa manyunyu ya mvua, 'Iweni manyunyu makubwa ya mvua.' 7 Huuzuia
mkono wa kila mtu usifanye kazi, ili kwamba watu wote aliowaumba wataona
matendo yake. 8 Kisha hayawani huenda na kujificha na kukaa katika mapango yake.
9 Dhoruba hutoka katika chumba chake upande wa kusini na baridi kutoka katika
pepo zilizotawanyika katika upande wa Kaskazini. 10 Barafu imetolewa kwa pumzi
ya Mungu; upana wa maji umeganda kama chuma. 11 Hakika, huyapima mawingu
manene yenye unyevu; yeye huusambaza mwanga wake katika mawingu. 12 Yeye
huyazungusha mawingu kwa uongozi wake, ili yafanye chochote anayoyaagiza juu ya
uso wote wa ulimwengu. 13 Huyafanya haya yote yatokee; wakati mwingine hutokea
kwa ajili ya kusahihisha, wakati mwingine kwa ajili ya nchi yake, na wakati mwingine
ni kwa matendo ya agano la uaminifu. 14 Yasikilize haya, Ayubu; acha na ufikiri juu
matendo ya ajabu ya Mungu. 15 Je unajua ni kwa namna gani Mungu hushurutisha
mawingu na kuufanya mwanga wa radi ung'ae ndani yake? 16 Je unafahamu
kuelea kwa mawingu, matendo ya ajabu ya Mungu, Je ni nani aliyemkamilifu katika
maarifa? 17 Je unafahamu ni kwa jinsi gani mavazi yako huwa ya moto wakati nchi

ikiwa imetulia kwasababu ya upepo unaotoka upande wa kusini? [18] Je unaweza
kulitandaza anga kama anavyofanya - anga ambalo lina nguvu kama kioo cha chuma
kigumu? [19] Tufundishe sisi kile tunachopaswa kumwambia yeye, kwa kuwa hatuwezi
kutoa hoja zetu katika mpangilio kwasababu ya kiza katika akili zetu. [20] Je anapaswa
kuambiwa kwamba ninapenda kuongea naye? Je mtu angependa kumezwa? [21] Sasa,
watu hawawezi kulitazama jua wakati linang'aa katika anga baada ya upepo kupita
katikati yake na umelisafisha kwa mawingu yake. [22] Kutoka upande wa kaskazini
hutokea fahari ya dhahabu - juu ya Mungu kuna ukuu wa kutisha. [23] Na kuhusu
Mwenye nguvu, hatuwezi kumpata; yeye ni mkuu katika nguvu na haki. Yeye hatesi
watu. [24] Hivyo basi, watu humwogopa. Yeye huwa hawajali wale ambao ni wenye
hekima katika akili zao wenyewe."

# 38

[1] Ndipo Yahweh alimwita Ayubu kutoka katika dhoruba kali na kumwambia,
[2] "Huyu ni nani aletaye giza katika mipango kwa njia ya maneno bila maarifa?
[3] Basi sasa jifunge kiunoni mwako kama mwanaume kwa kuwa nitakuuliza maswali,
nawe lazima unijibu. [4] Wewe ulikuwa wapi wakati nilipoitandaza misingi ya
dunia? Niambie, kama unao ufahamu zaidi. [5] Je ni nani aliyeamuru vipimo
vyake? Niambie, kama unajua, ni nani alivinyosha vipimo juu yake? [6] Misingi
yake ilitandazwa juu ya nini? Ni nani aliyeliweka jiwe lake la pembeni [7] wakati
nyota za asubuhi zilipoimba pamoja na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa
furaha? [8] Ni nani huifunga bahari kwa milango wakati inapofurika, kana kwamba
inatoka katika tumbo, [9] wakati nilipoyafanya mawingu kuwa ni mavazi yake, na giza
nene kuwa mkanda wake wa kujifungia? [10] Hapo ilikuwa wakati nilipoweka bahari
mpaka wangu, na nilipoweka makomeo yake na milango, [11] na wakati nilipoiambia,
'Unaweza kuja hapa kutoka mbali, lakini si zaidi; na hapa ndipo nitauweka mpaka
kwa fahari ya mawimbi yako.' [12] Je tangu mwanzo wa siku zako, ulishawahi kuigiza
asubuhi ianze, na kuyafanya mapambazuko yajue sehemu yake katika mpangilio
wa vitu, [13] ili kwamba ishikilie sehemu za dunia ili watu waovu watikiswe mbali
nayo. [14] Dunia imebadilishwa katika mwonekano kama udongo unavyobadilika chini
ya muhuri; vitu vyote husimama juu yake dhahiri kama cha kibindo cha nguo.
[15] 'Mwanga' wao umeondolewa kutoka kwa watu waovu; na mkono wao ulioinuliwa
umevunjwa. [16] Je umeshaenda kwenye vyanzo vya maji ya bahari? Je umeshatembea
sehemu za chini kabisa za kilindi? [17] Je malango ya mauti yamefunuliwa kwako? Je
umeshaona malango ya uvuli wa mauti? [18] Je umeifahamu dunia katika upana wake?
Niambie kama unayajua yote hayo. [19] Je iko wapi njia ya sehemu ya kupumzikia kwa
mwanga, na kama ilivyo kwa giza, iko wapi sehemu yake? [20] Je unaweza kuuongoza
mwanga na giza katika sehemu zake za kazi? Waweza kuitambua njia ya kurudi
katika nyumba zao? [21] Bila shaka unajua, kwa kuwa ulizaliwa wakati huo; hesabu
ya siku zako ni kubwa sana! [22] Je ulishaingia katika ghala ya barafu, au umeshaiona
ghala ya mawe ya mvua, [23] vitu hivi nimeviweka kwa ajili ya siku za mateso, kwa siku
za mapigano na vita? [24] Je iko wapi njia ya mshindo wa mwanga hutokea au je upepo
husambazwa kutoka mashariki juu ya dunia? [25] Ni nani aliyezitengeneza mifereji ya
gharika ya mvua, au ni nani aliyezifanya njia za milipuko ya radi, [26] na kuifanya
mvua inyeshe juu ya nchi ambazo hakuna mtu aishiye ndani yake, na juu ya jangwa,
ambayo ndani yake hakuna mtu yeyote, [27] kwa kusudi la kutimiza mahitaji ya mikoa
iliyo kame na yenye ukiwa, na kuyastawisha majani mororo? [28] Je kuna baba wa
mvua? Ni nani aliyeyafanya matone ya umande? [29] Je barafu ilitoka katika tumbo
la nani? Na ni nani aliyeizaa theluji nyeupe katika anga? [30] Maji hujificha menyewe
na kuwa kama jiwe; sehemu za juu za vilindi huwa kama barafu. [31] Je unaweza

kuzifunga minyororo ya Kilimia, au kuvifungua vifundo vya Orioni? 32 Je unaweza kuziongoza nyota kutokea katika nyakati zake? Je waweza kuongoza dubu pamoja na watoto wake? 33 Je unazijua sheria za anga? Wewe uliweza kuanzisha sheria za anga juu ya dunia? 34 Je waweza kupaza sauti yako hadi mawinguni, ili kwamba maji mengi ya mvua yakufunike? 35 Je waweza kuagiza miali ya mwanga ili itokee, na kukwambia, 'Sisi tupo hapa'? 36 Ni nani ameweka hekima katika mawingu au ni nani ameweka ufahamu kwa ukungu? 37 Nani anaweza kuyahesabu mawingu kwa maarifa yake? Na ni nani awezaye kuvimwaga viriba vya anga 38 wakati mavumbi yanapoungana kuwa kitu kigumu na mabonge ya dunia yanaposhikama kwa pamoja?
39 Je waweza kuwinda mawindo kwa ajili ya simba jike au kutosheleza hamu ya watoto wadogo wa simba 40 wakati wanapokwaruza kwaruza katika pango lao na kukaa katika kificho ili kulala katika hali ya kuvizia? 41 Ni nani aletaye mawindo kwa ajili ya kunguru wakati ambapo watoto wao wanapomlilia Mungu na kutangatanga kwa kukosa chakula?

# 39

1 Je unajua ni wakati gani mbuzi mwitu huzaa watoto wao katika miamba? Je
waweza kuwangalia paa wakati wanapozaa watoto wao? 2 Waweza kuhesabu miezi
ya kuchukua mimba? Je unaujua muda ambao huzaa watoto wao? 3 Wanainama
chini na kuzaa watoto wao, na kisha maumivu yao ya uzazi yanaishi. 4 Watoto
wao huwa na nguvu na kukua katika uwanda wa wazi; hutoka nje na hawarudi
tena. 5 Ni nani huwaacha punda mwitu waende huru? Je nani amevilegeza vifungo
vya punda wepesi, 6 ni nyumba ya nani nimeifanya katika Araba, au nyumba yake
katika nchi ya chumvi? 7 Hucheka kwa dharau katika kelele katika mji; hasikilizi
kelele za mwongozaji. 8 Hutembeatembea juu ya milima kama malisho yake; huko
hutafuta kila mmea ulio wa kijani kwa ajili ya kula. 9 Je nyati atakuwa na furaha
kukutumikia? Je atakubali kukaa katika zizi lako? 10 Waweza kumwongoza nyati
kulima mtaro kwa kamba? Je atachimba bonde kwa ajili yako? 11 Je waweza
kumtumaini kwasababu ya nguvu zake nyingi? Je waweza kumwachia kazi yako
ili aifanye? 12 Je waweza kumtegemea akuletee nyumbani nafaka, au kukusanya
nafaka katika uwanda wako wa kupuria? 13 Mabawa ya mbuni hupunga kwa
majivuno, bali je mabawa na manyoya yana upendo? 14 Kwa maana huuacha mayai
yake katika nchi, na huyaacha yapate joto katika mavumbi; 15 husahau kuwa mguu
waweza kuyaharibu au kwamba mnyama mwitu aweza kuyakanyaga. 16 Huyatendea
vibaya makinda yake kana kwamba si yake; haogopi kwamba kazi yake yaweza
kupotea bure, 17 kwasababu Mungu amemnyima hekima na hajampa ufahamu
wowote. 18 Na wakati anapokimbia kwa haraka, huwacheka kwa dharau farasi na
mpanda farasi wake. 19 Je umempa farasi nguvu zake? Je umeivika shingo yake
kwa manyoya? 20 Je umemfanya aruke kama panzi? Enzi ya mlio wake ni wa
kutisha. 21 Hurarua kwa nguvu na kufurahia katika nguvu zake; hukimbia upesi
kukutana na silaha. 22 Huidharau hofu na hashangazwi; huwa harudi nyuma kutoka
katika upanga. 23 Podo hugongagonga ubavuni mwake, pamoja na mkuki unaong'aa
na fumo. 24 Huimeza nchi kwa hasira na ghadhabu; katika sauti ya tarumbeta,
hawezi kusimama sehemu moja. 25 Wakati wowote tarumbeta inapolia, husema,
'Ooh! Huisikia harufu ya vita kutoka mbali - vishindo vya radi za makamanda
na makelele. 26 Je ni kwa hekima yako kwamba mwewe hupaa juu, na ya kuwa
huyanyosha mabawa yake kwa upande wa kusini? 27 Je ni kwa agizo lako kwamba tai
huruka juu na kufanya kiota chake katika sehemu za juu? 28 Huishi katika majabali
na hufanya makao yake katika vilele vya majabali, na ngomeni. 29 Kutoka huko

hutafuta mawindo; macho yake huyaona mawindo kutoka mbali. 30 Makinda yake
hunywa damu pia; na pale walipo watu wafu, ndipo na yeye alipo.

# 40

1 Yahweh aliendelea kuongea na Ayubu na kusema, 2 "Je mtu yeyote anayetaka
kukosoa na ajaribu kumsahihisha Mwenye enzi? Na yeye anayehojiana na Mungu,
na ajibu yeye." 3 Ndipo Ayubu akamjibu Yahweh na kusema, " 4 Tazama, mimi si mtu
muhimu; je nawezaje kukujibu? Ninauweka mkono wangu juu ya mdomo wangu.
5 Ninazungumza mara moja, na sitakujibu; hakika, mara mbili, lakini sitaendelea
zaidi." 6 Kisha Yahweh akamjibu Ayubu kutoka katika dhoruba kali na kusema,
7 "Jifunge sasa mkanda kiunoni mwako kama mwanaume, kwa kuwa nitakuuliza
maswali, nawe lazima unijibu. 8 Je waweza kusema kwa hakika kwamba mimi
si mwenye haki? Je utanihukumu mimi ili useme wewe ni mwenye haki? 9 Je
una mkono kama wa Mungu? Je waweza kutoa kishindo kwa sauti kama yeye?
10 Jivike sasa katika utukufu na katika utu; jivalie mwenyewe heshima na enzi.
11 Sambaza ziada ya hasira yako; mtazame kila mmoja mwenye kiburi na umshushe
chini. 12 Mwangalie kila mmoja mwenye kiburi na umweke chini; wakanyage chini
watu waovu mahali wanaposimama. 13 Wazike ardhini pamoja; zifunge nyuso
zao katika sehemu zilizositirika. 14 Ndipo pia nitakapokubali ya kwamba mkono
wako wa kulia waweza kukuokoa. 15 Mwangalie sasa kiboko, ambaye niliwafanya
kama nilivyokufanya wewe; anakula nyasi kama ng'ombe. 16 Ona sasa, nguvu zake
ziko katika viuno vyake; nguvu zake zi katika mishipa ya tumbo lake. 17 Yeye
huuondoa mkia wake kama mti wa mwerezi; mishipa ya paja lake imeunganishwa
pamoja. 18 Mifupa yake ni kama ya mirija ya shaba; na miguu yake ni kama
kipande cha chuma. 19 Yeye ni mkuu wa viumbe vya Mungu. Ni Mungu pekee,
ambaye alimwumba, anaweza kumshinda. 20 Kwa kuwa milima humpatia chakula;
hayawani wa mashambani hucheza karibu. 21 Hujilaza chini ya mimiea ya kivuli
katika makao ya mianzi, na katika bwawa la matope. 22 Miti yenye vivuli humfunika
katika vivuli vyake; mierebi ya kijito inamzunguka pande zote. 23 Tazama, kama mto
utazigharikisha kingo zake, hatikisiki; yeye anajiamini, hata kama Mto wa Yordani
unajaa hadi katika pua yake. 24 Je mtu yeyote aweza kumnasa kwa ndoano, au
kuichoma pua yake kwa mtego?

# 41

1 Je waweza kumvua mamba kwa ndoano ya samaki? Au kumfunga taya zake kwa
kamba? 2 Je waweza kuweka kamba katika pua zake, au kumtoboa taya yake kwa
ndoano? 3 Je atafanya maombi mengi kwako? Je atazungumza na wewe kwa maneno
laini? 4 Je atafanya agano na wewe, ili kwamba umchukue kwa ajili ya mtumishi
milele? 5 Je utacheza pamoja naye kama ambavyo ungecheza na ndege? Je utamfunga
kwa ajili ya mtumishi wako wa kike? 6 Je makundi ya wavuvi waweza kumfanyia
biashara? Je watamgawanya ili kufanya biashara miongoni mwa wafanya biashara?
7 Je waweza kuijaza ngozi yake kwa vyusa au kichwa chake kwa mikuki ya kuvulia?
8 Weka mkono wako juu yake mara moja, nawe utaikumbuka vita na hautaendelea
kufanya hivyo tena. 9 Tazama, matumaini ya kila mtu ambaye hufanya hivyo ni
uongo; je si kila mmoja atatupwa chini katika nchi mbele yake? 10 Hakuna aliye
mkali ambaye aweza kuthubutu kumtikisa mamba; Ni nani basi awezaye kusimama
mbele yake? 11 Ni nani kwanza aliyenipa kitu chochote ili kwamba niweze kumlipa?
Chochote kilicho chini ya anga ni changu. 12 Sitanyamaza kimya kuhusu miguu ya
mamba, wala kuhusu jambo linalohusu nguvu zake, wala kuhusu umbo lake zuri.
13 Nani awezaye kuiondoa ngozi yake? Nani anaweza kumchoma kwa silaha mara

mbili? 14 Nani awezaye kuifungua milango ya uso wake, imezungukwa na meno
yake ambayo yanaogofya? 15 Mgongo wake umefanywa kwa magamba yenye mistari,
yamefungwa kwa pamoja kama chapa. 16 Moja li karibu na jingine na ya kuwa
hakuna hewa inaweza kupita katikati yake. 17 Yameunganishwa moja kwa jingine;
yamegandamana kwa pamoja, ili kwamba hayawezi kutenganishwa. 18 Mwanga
hung'ara kutoka katika kupumua kwake; macho yake ni kama kope za mapambazuko
ya asubuhi. 19 Ndani ya mdomo wake hutoka miali ya mwanga, chembe za moto
huruka nje. 20 Katika pua zake hutoka moshi kama chungu kinachotokota juu ya
moto ambao umechochewa ili uwe na joto sana. 21 Pumzi yake huwasha mkaa
na kuwa mwali; moto hutoka katika mdomo wake. 22 Katika shingo yake kuna
nguvu, na kitisho hucheza mbele yake. 23 Nofu za mwili wake zimeunganishwa
pamoja; ziko imara katika yeye; wala haziwezi kuondolewa. 24 Moyo wake ni mgumu
kama jiwe - hakika, ni mgumu kama jiwe la chini la kusagia. 25 Na anaposimama
mwenyewe, hata miungu huogopa; hurudi nyuma kwasababu ya hofu. 26 Na ikiwa
atapigwa kwa upanga, hauwezi kumfanya kitu chochote, wala mkuki, wala mshale,
wala aina yoyote ya silaha iliyochongoka. 27 Yeye hufikiri juu ya chuma kana
kwamba ni majani makavu na hufikiri juu ya fedha kana kwamba ni ubao uliooza.
28 Mshale hauwezi akamfanya akimbie; kwake yeye mawe ya kombeo huwa kama
makapi. 29 Marungu huyaangalia kama majani makavu; yeye hucheka juu ya mkuki
unaovuma. 30 Sehemu zake za chini zi kama vipande vilivyochongoka vya vyungu;
huacha alama zilizosambaa katika udongo kana kwamba alikuwa ni chombo cha
kusagia. 31 Yeye hukifanya kilindi kichemke kama chungu cha maji ya moto; huifanya
bahari kama chungu cha lihamu. 32 Yeye huifanya njia ing'are nyuma yake; mtu
mmoja angedhani kilindi kuwa cheupe. 33 Hakuna cha kumlinganisha juu ya dunia,
ambaye yeye alikuwa ameumbwa kuishi pasipo hofu. 34 Hukiona kila kitu chenye
kiburi; yeye ni mfalme juu ya wana wote wa kiburi."

# 42

1 Kisha Ayubu akamjibu Yahweh na kusema, 2 "Ninajua kwamba unaweza kufanya
mambo yote, ya kuwa hakuna kusudi lako linaweza kuzuiliwa. 3 Ni nani huyo
ambaye pasipo maarifa huificha mipango? Kwa kweli nilisema mambo ambayo
sikuyaelewa, mambo magumu kwangu kuyafahamu, ambayo juu yake sikujua
chochote. 4 Uliniambia, 'Sikiliza sasa, nami nitasema; nitakuuliza mambo, nawe
utaniambia.' 5 Nimekuwa nikikusikia kwa usikivu wa sikio langu, lakini sasa jicho
langu linakuona wewe. 6 Basi ninajidharau mwenyewe; ninatubu kwa mavumbi na
majivu." 7 Ilitokea baada ya kuwa amekwisha kusema maneno hata kwa Ayubu,
Yahweh alimwambia Elifazi Mtemani, " Ghadhabu yangu imewaka dhidi yako na
dhidi ya marafiki zako wawili kwa kuwa hamkusema maneno ya haki juu yangu
kama alivyofanya mtumishi wangu Ayubu. 8 Sasa basi, jitwalieni mafahari saba
na mabeberu saba, kisha mmwendee mtumishi wangu Ayubu na mtoe sadaka ya
kuteketezwa kwa ajili yenu. Ndipo Mtumishi wangu Ayubu atawaombea ninyi, nami
nitayapokea maombi yake, ili kwamba nisiwashughulikie sawasawa na upumbavu
wenu. Maana hamkusema mambo ya haki juu yangu, kama alivyofanya mtumishi
wangu Ayubu." 9 Basi Elifazi Mtemani, Bildadi Mshuhi na Zofari Mnaamathi walienda
na kufanya kama vile Yahweh alivyowaamuru, na Mungu alimtakabali Ayubu. 10 Na
wakati Ayubu alimpowaombea rafiki zake, Yahweh alirejeza bahati yake. Yahweh
alimjalia mara mbili ya kile alichokimiliki hapo awali. 11 Ndipo ndugu zake na Ayubu,
na wale jamaa zake wote walikuwa wanajuana naye hapo mwanzo, walikuja hapo
kwake na kula chakula pamoja naye katika nyumba yake. Waliomboleza pamoja
naye na walimfariji kwa ajili majanga yote ambayo Yahweh alikuwa ameyaleta juu

yake. Kila mtu alimpa Ayubu kipande cha fedha na pete ya dhahabu. 12 Yahweh
aliubarikiwa mwisho wa maisha ya Ayubu kuliko mwanzo wake; alikuwa na kondoo
kumi na nne elfu, ngamia elfu sita, jozi elfu moja, na punda jike elfu moja. 13 Pia
alikuwa na wana saba na mabinti watatu. 14 Binti wa kwanza alimwita Yemima,
na wa pili Kezia, na wa tatu Kerenihapuki. 15 Katika nchi yote hawakupatikana
wanawake wazuri kama mabinti wa Ayubu. Baba yao aliwapa urithi miongoni mwa
kaka zao. 16 Baada ya haya, Ayubu aliishi miaka 140; aliwaona wana wake na wana
wa wanawe, hata kizazi cha nne. 17 Basi Ayubu alifariki, akiwa mzee na akijawa na
siku nyingi.

# Zaburi

## 1

1 Amebarikiwa mtu yule asiye enenda katika ushauri wa waovu, au kusimama
katika njia ya wenye dhambi, au kukaa katika kusanyiko la wenye mizaha. 2 Bali yeye
huifurahia sheria ya Yahwe, na huitafakari sheria yake mchana na usiku. 3 Atakuwa
kama mti uliopandwa karibu na mkondo wa maji ambao huzaa matunda yake kwa
majira yake, ambao majani yake hayakauki; lolote afanyalo litafanikiwa. 4 Waovu
hawako hivyo, wao badala yake ni kama makapi yapeperushwayo na upepo. 5 Kwa
hivyo waovu hawatasimama katika hukumu, wala wenye dhambi katika kusanyiko
la wenye haki. 6 Kwa kuwa Yahweh huikubali njia ya wenye haki, njia ya waovu
itaangamizwa.

## 2

1 Kwa nini mataifa wanafanya dhoruba, kwa nini watu wanafanya njama ambazo
zitafeli? 2 Wafalme wa nchi kwa pamoja hushikilia misimamo yao na watawala kwa
pamoja hufanya njama kinyume na Yahwe na kinyume na Masihi, wakisema, 3 "Ngoja
tuzikate pingu walizo tufingia sisi na kuzitupa pingu zao." 4 Yeye aketie katika mbingu
atacheka kwa dharau mbele yao; Bwana atawadhihaki wao. 5 Kisha ataongea nao
katika hasira yake na kuwaogofya kwa gadhabu yake, akisema, 6 "Mimi mwenyewe
nilimpaka mafuta mfalme wa Sayuni, mlima wangu mtakatifu." 7 Nami nitatangaza
amri ya Yahwe. Yeye aliniambia, "wewe ni mwanangu! Leo hii nimekuwa baba
yako. 8 Uniombe, nami nitakupa wewe taifa kwa ajili ya urithi na mikoa ya nchi iliyo
bora kwa ajili ya umiliki wako. 9 Wewe utawavunja wao kwa fimbo ya chuma; kama
vile mtungi wa mfinyanzi, wewe utawavunja wao vipande vipande." 10 Hivyo sasa,
ninyi wafalme; mchukue tahadhari; mjirekebishe. 11 Mwabuduni Yahwe kwa hofu na
mfurahi mkitetemeka. 12 Mumbusu mwana vinginevyo atawakasirikia, na mtakufa
pale pale hasira yake ikiwaka. Ni jinsi gani wamebarikiwa wale wote watafutao
usalama ndani yake.

## 3

Zaburi ya Daudi, wakati alipo mkimbia mtoto wake Absalom. 1 Yahewh, maadui
zangu wako wangapi! Ni wengi wamekuja kinyume na mimi. 2 Ni wengi
wanaonisema, "Hakuna msaada wowote kutoka kwa Mungu kwa ajili yake." Selah
3 Bali wewe, Yahweh, u ngao yangu pande zote, utukufu wangu, na uniinuaye kichwa
changu. 4 Nampazia Yahweh sauti yangu, na yeye ananijibu kutoka katika mlima
wake mtakatifu. 5 Nilijilaza chini na kusinzia; na niliamka, kwa kuwa Yahweh
alinilinda. 6 Sitaogopa kusanyiko la watu ambao wamejipanga kinyume na mimi
pande zote. 7 Inuka, Yahweh! Uniokoe, Mungu wangu! Kwa kuwa utawapiga maadui
zangu wote kwenye taya zao; utayavunja meno ya waovu. 8 Wokovu unatoka kwa
Yahweh. Baraka zako ziwe juu ya watu wako.

## 4

Kwa kiongozi wa muziki; kwenye vyombo vya nyuzi. Zaburi ya Daudi. 1 Unijibu
nikuitapo, Mungu wa haki yangu; uniokoe niwapo katika hatari. Unihurumie na
usikie maombi yangu. 2 Ninyi watu, mpaka lini mtaiabisha heshima yangu? Mpaka
lini mtaendelea kupenda kile kisicho stahili na kutafuta uongo? 3 Lakini mjue ya
kuwa Yahweh huchagua watu wa kimungu kwa ajili yake. Nitakapo mwita Yahwe

atasikia. 4 Tetemekeni na kuogopa, lakini msitende dhambi! Tafakarini mioyoni
mwenu kwenye vitanda vyenu na muwe kimya. 5 Toeni matoleo ya haki na muweke
imani yenu katika Yahweh. 6 Wengi husema, “Ni nani atakaye tuonyesha chochote
kilicho kizuri?” Yahweh, utuangazie nuru ya uso wako. 7 Umeupa moyo wangu
furaha kuu kuliko wao wanapozidishiwa nafaka na divai mpaya. 8 Ni amani kuwa
nitajilaza na kusinzia, kwako pekee, Yahweh, nifanye kuwa salama kabisa.

# 5

Kwa kiongozi wa muziki; kwa vyombo vya upepo. Zaburi ya Daudi. 1 Sikiliza
nikuitapo, Yahweh; tazama kuugua kwangu. 2 Sikiliza sauti yangu nikuitapo, Ee
Mfalme wangu na Mungu wangu, kwa kuwa ni kwako Bwana naomba. 3 Yahweh;
sikia kilio changu asubuhi; na asubuhi nitaleta dua yangu kwako na kungoja kwa
matarajio. 4 Hakika wewe ni Mungu usiye kubaliana na uovu; watu waovu hawawezi
kuwa wageni wako. 5 Wenye kiburi hawata simama katika uwepo wako; wewe
unawachukia wote wanaofanya maovu. 6 Nawe utawaharibu waongo; Yahweh
huwadharau vurugu na watu wadanganyifu. 7 Lakini kwangu mimi, kwa sababu
ya ukuu na uaminifu wa agano lako, nitakuja nyumbani mwako; na kwa heshima
nitakuinamia mbele ya hekalu lako takatifu. 8 Oh Bwana, uniongoze katika haki
yako kwa sababu ya adui zangu; usawazishe njia yako mbele yangu. 9 Kwa kuwa
midomoni mwao hamna ukweli; utu wao wa ndani ni mwovu; makoo yao ni kaburi
lililo wazi; husifu kinafiki kwa ulimi wao. 10 Mungu, wafanye kuwa na hatia; mipango
yao iwe kuanguka kwao! Kwa ajili ya makosa yao mengi uwatoe nje, kwa kuwa
wamekuasi wewe. 11 Bali wale wanao kukimbilia wafurahi; uwafanye wapige kelele
kwa shangwe siku zote kwa sababu unawapigania; uwafanye wenye furaha ndani
yako, wale walipendao jina lako. 12 Kwa maana utawabariki wenye haki, Yahweh;
utawazunguka kwa neema kama ngao.

# 6

Kwa kiongozi wa muziki; kwenye vyombo vya nyuzi, weka kwenye mtindo wa
Sheminith. Zaburi ya Daudi. 1 Yahweh, usinikemee ukiwa na hasira au usiniadhibu
katika gadhabu yako. 2 Unihurumie, Yahwe, kwa maana ni dhaifu; uniponye, Yahweh,
kwa kuwa mifupa yangu ina tikisika. 3 Moyo wangu pia umesumbuka sana. Lakini
wewe, Yahweh, mpaka lini hali hii itaendelea? 4 Rudi, Yahweh! uniokoe. Uniokoe
kwa sababu ya uaminifu wa agano lako! 5 kwa kuwa kifoni hakuna kumbukumbu
lako. Kuzimuni ni nani atakaye kushukuru? 6 Nimechoshwa na kuugua kwangu.
Ninalowanisha kitanda changu kwa machozi usiku kucha; ninaosha kiti changu kwa
machozi. 7 Macho yangu yanafifia kwa kulia sana; yanazidi kuwa dhaifu kwa sababu
ya adaui zangu. 8 Ondokeni kwangu, nyote mtendao maovu; kwa kuwa Yahweh
amesikia sauti ya kilio changu. 9 Yahweh amesikia malalamiko yangu kwa ajili ya
huruma; Yahweh ameyapokea maombi yangu. 10 Maadui zangu wote wataaibishwa
na kuteswa sana. Watarudi nyuma na ghafra kufedheheshwa.

# 7

Utungo wa muziki wa daudi, ambao alimwimbia Yahwe kuhusu maneno ya Cush
Mbenjamini 1 Yahweh Mungu wangu, kwako napata kimbilio! Uninusuru na hao wote
wanikimbizao, na uniokoe. 2 Vinginevyo, watanipura kama simba, na kunitawanya
viapande vipande na asiwepo mtu wa kuweza kunirudisha katika usalama. 3 Yawheh
Mungu wangu, Sijawahi kufanya kile maadui zangu wanacho sema nilifanya; sina
hatia katika mikono yangu. 4 Sijawahi kumkosea mtu yeyote aliye na amani na
mimi, au kumdhuru kipumbavu yeyote aliye kinyume na mimi. 5 Ikiwa sisemi

ukweli basi umruhusu adui yangu kuyaingilia maisha yangu na kuyaharibu; na
umuache aukanyage mwili wangu ulio hai kwenye aridhi na kuuacha umelala kwa
aibu mavumbini. Selah 6 Inuka, Yahweh, katika hasira yako; simama kinyume
na hasira kali ya adui zangu; amka kwa ajili yangu na ubebe amri zako ambazo
wewe umeamuru kwa ajili yao. 7 Mataifa yote yamekuzunguka; uwatawale kutoka
mbinguni. 8 Yahweh, uwahukumu mataifa; uwaonyeshe kuwa sina hatia, Yahweh,
kwa sababu mimi ni mwenye haki na sina hatia, Ewe uliye juu. 9 Matendo ya
waovu na yafike mwisho, bali uanzishe watu wenye haki, Mungu mwenye haki, wewe
ambaye unapima mioyo na fahamu. 10 Ngao yangu inatoka kwa Mungu, yule anaye
okoa moyo wa mwenye haki. 11 Mungu ni mwamuzi mwenye haki, Mungu anaye
chukizwa na waovu kila siku. 12 Ikiwa kuna mtu hatubu, Mungu atanoa upanga
wake na ata andaa upinde wake kwa ajili ya vita. 13 Ana jiandaa kutumia siraha
kupambana naye; anatengeneza mishale yake kuwa ya moto. 14 Fikiria kuhusu huyo
ambaye ana ujauzito wa maovu, mwenye mimba ya mipango ya uharibifu, anaye
zaa sumu ya uharibifu. 15 Yeye huchimba shimo na kuliacha wazi kisha baadaye
hudumbukia katika shimo alilochimba mwenyewe. 16 Mipango yake mwenyewe ya
uharibifu hugeukia kichwa chake mwenyewe, kwa kuwa vurugu zake mwenyewe
humshukia kichwani pake. 17 Kwa haki yako Mungu nitakushukuru; nitaimba sifa
kwa Mungu aliye juu.

# 8

Kwa kiongozi wa muziki; weka kwenye mtindo wa gittith. Zaburi ya Daudi.
1 Yahweh Bwana wetu, ni jinsi gani jina lako ni tukufu katika dunia yote, wewe
ufunuaye utukufu wako juu mbinguni. 2 Kutoka katika midomo ya watoto na
vichanga umeumba sifa kwa sababu ya utukufu wako, ili kuwanyamazisha maadui
wote na walipa kisasi wote. 3 Ninapozitazama mbingu, ambazo vidole vyako
vimeumba, mwezi na nyota, ambazo umeziweka kila mmoja katika nafasi yake,
4 Binadamu ni nani hata umtazame, na watu hata uwajali wao? 5 Umewaumba
chini kidogo kuliko viumbe vya mbinguni na umewazunguka na utukufu na heshima.
6 Umemfanya binadamu kutawala kazi ya mikono yako; umeviweka vitu vyote chini
ya miguu yake: 7 kondoo na ng'ombe wote, na hata wanyama wa porini, 8 ndege
wa angani, na samaki wa baharini, na vyote vipitavyo katika mikondo ya bahari.
9 Yahweh Bwana wetu, ni jinsi gani jina lako ni tukufu katika dunia yote!

# 9

Kwa kiongozi wa muziki; weka kwenye mtindo wa Muth Labben. Zaburi ya Daudi.
1 Nitamshukuru Yahweh kwa moyo wangu wote; nitayasimulia matendo yako makuu.
2 Nitafurahi na kushangilia katika wewe; nitaliimbia jina lako, Wewe uliye juu.
3 Maadui zangu wanaponirudia, hujikwaa na kuangamia mbele zako. 4 Kwa kuwa
umenitetea kwa haki; unakaa kwenye kiti chako cha enzi, ukihukumu kwa haki!
5 Uliwakemea mataifa; umewaharibu waovu; na kuwa futilia mbali jina lao milele na
milele. 6 Maadui wamebomoka kama magofu ulipo pindua miji yao. Kumbukumbu
yao yote imepotea. 7 Bali Yahweh anadumu milele; ameweka kiti chake cha enzi kwa
ajili ya haki. 8 Naye atauhukumu ulimwengu kwa haki, na atatekeleza hukumu kwa
ajili ya mataifa kwa haki. 9 Yahweh pia atakuwa ngome kwake aliye onewa, na ngome
wakati wa shida. 10 Wale wakujuao jina lako wanaamini katika Wewe, kwa ajili yako,
Yahweh, usiwaache wale wakutafutao. 11 Mwibieni sifa Yahweh, anaye tawala katika
Sayuni; waambieni mataifa yale aliyo yatenda. 12 Kwa kuwa Mungu alipizae kisasi
cha damu hukumbuka; naye hasahau kilio cha anayeonewa. 13 Unihurumie, Yahweh;
tazama vile ninavyo onewa na wale wanao nichukia, wewe ambaye unaweza

kunikwapua katika lango la kifo. [14] Oh, ili niweze kutangaza sifa zako. Katika lango
la binti sayuni nitaufurahia wokovu wako! [15] Mataifa yamedidimia chini katika
shimo ambalo walilolitengeneza; miguu yao imenaswa kwenye nyavu walioificha
wenyewe. [16] Yahweh amejidhihilisha; na kutekeleza hukumu; waovu wameangamia
kwa matendo yao wenyewe. Selah [17] Waovu wamekataliwa na kupelekwa kuzimu,
mataifa yote yanayo msahau Mungu. [18] Kwa kuwa mhitaji hata sahauliwa siku zote,
wala matumaini ya wanyonge hayatapotea milele. [19] Inuka, Yahweh, usimruhusu mtu
kutushinda; mataifa na wahukumiwe mbele zako. [20] Bwana, waogopeshe; mataifa
waweze kutambua kuwa ni wanadamu tu. Selah

# 10

[1] Kwa nini, Yahweh, unasimama mbali? Kwa nini unajificha wakati wa shida?
[2] Kwa sababu ya majivuno yao, watu waovu waawakimbiza wanyonge; Basi tafadhari
uwafanye waovu kunaswa kwa mipango yao wenyewe walioipanga. [3] Kwa kuwa mtu
mwovu hujivuna kwa tamaa yake ya ndani; yeye hufurahisha tamaa na kumtusi
Yahweh. [4] Mtu mwovu ameinua uso wake; naye hamtafuti Mungu. Yeye hamfikilii
Mungu kamwe kwa kuwa hamjali kabisa Mungu. [5] Yeye yuko salama wakati wote,
amri zako za haki ziko juu sana kwake; naye huwadharau adui zake wote. [6] Yeye
husema moyoni mwake, “Siwezi kamwe kushindwa; katika kizazi chote sitakutana
na shida.” [7] Mdomoni mwake kumejaa kulaani na udanganyifu, maneno yenye
sumu; ulimi wake unajeruhi na kuharibu. [8] Yeye husubilia kwenye shambulio karibu
na kijiji; mahali pa siri huwauwa watu wasio na hatia; macho yake huwatazama
wasionahatia. [9] Hujibanza mahari pa siri kama simba katika kichaka; yeye hulala
akisubiri kumkamata mnyonge. Humkamata pale anapokwisha mweka mtegoni
mwake. [10] Wanyonge wake hugandamizwa chini na kupigwa; wao huangukia katika
mtego imara. [11] Yeye husema katika moyo wake, “Mungu amesahau; huficha uso
wake; hawezi kujishughulisha kutazama.” [12] Inuka, Yahweh! Inua mkono wako,
Mungu! Usiwasahau wanyonge. [13] Kwa nini mtu mwovu anamkataa Mungu na
kusema moyoni mwake, “Hautanipata katika hatia?” [14] Umeona, maana mara zote
unaangalia mtu aletaye madhara na jeuri. Mtu asiye na msaada hukuachia nafsi
yake; maana wewe huwaokoa yatima. [15] vunja mkono wa mwovu lo na mtu mwovu.
Umuajibishe kwa matendo yake maovu, ambayo kwayo alifikiri hautayagundua.
[16] Yahweh ni mfalme milele daima; mataifa yanaondolewa katika aridhi yake.
[17] Yahweh, umesikia uhitaji wa wanyonge; nawe umeitia nguvu mioyo yao, wewe
unasikia maombi; [18] Unawatetea yatima na wanyonge ili kusudi pasiwepo na mtu
katika dunia hii atakaye leta hofu tena.

# 11

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya daudi. [1] Ni kwako Yahweh ninapata usalama;
ni kwa namna gani utasema na mimi, “Ruka kama ndege hadi mlimani”? [2] Tazama!
Waovu wana andaa pinde zao. Wana tayarisha gizani mishale yao kwenye kamba ili
kufyatua mioyo ya wenye haki. [3] Ikiwa misingi imeharibiwa, mwenye haki atafanya
nini? [4] Yahweh yuko katika hekalu takatifu; macho yake yanatazama, yakiuchunguza
ubinadamu. [5] Yahweh huwachunguza wote wenye haki na waovu, bali huwachukia
wapendao kuwaumiza wengine. [6] Yeye huwanyeshea waovu makaa ya mawe na
moto wa jehanamu; upepo uunguzao utakuwa ni sehemu yao kutoka katika kikombe
chake! [7] Kwa kuwa Yahweh ni mwenye haki, Naye hupenda haki; wenye haki
watauona uso wake.

# 12

Kwa kiongozi wa muziki; weka kwenye Sheminith. Zaburi ya Daudi. 1 Msaada,
Yahweh, kwa kuwa wacha Mungu wametoweka; nao waaminifu wametokomea.
2 Kila mmoja anasema kwa jirani yake maneno matupu; kila mmoja anaongea kwa
midomo yenye sifa za uongo na maneno ya udanganyifu. 3 Yahweh, katilia mbali
midomo yenye sifa za uongo, kila ulimi unanena kwa nguvu mambo makubwa.
4 Hawa ni wale ambao wamesema, “Kwa ndimi zetu tutashinda. Wakati midomo yetu
itakapo ongea, ni nani atakaye kuwa mtawala juu yetu?” 5 “Kwa sababu ya vurugu
zilizopo kinyume na maskini, na kwa sababu ya kuugua kwao wahitaji, Nitainuka,”
asema Yahwe. “Nitawaletea usalama wanao hitaji.” 6 Maneno ya Yahwe ni masafi,
kama fedha iliyo safishwa katika tanuru duniani, iliyo ng'arishwa mara saba zaidi.
7 Wewe ni Yahwe! Unaye watunza. Una wahifadhi wacha Mungu kutoka katika
hiki kizazi cha waovu na hata milele. 8 Waovu hutembea kila pande pale uovu
unapoinuliwa kati ya wanadamu.

# 13

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi. 1 Mpaka lini, Yahweh, utaendelea
kunisahau? Ni kwa muda gani utauficha uso wako nisiuone? 2 Ni kwa muda gani
nitalazimika kuhofu na kuhuzunika moyoni mwangu kila siku? Ni kwa muda gani
adui zangu watanishida? 3 Unitazame na unijibu, Yahwe Mungu wangu! Nipe
mwanga machoni pangu, vinginevyo nitalala katika mauti. 4 Usimuache adui yangu
aseme, “Nimemshinda huyu,” ili kwamba asiweze kusema, “Nimemtawala adui
yangu;” la sivyo, maadui zangu watafurahia nitakapo shushwa chini. 5 Lakini
nimeamini katika uaminifu wa agano lako; moyo wangu wafurahia katika wokovu
wako. 6 Nitamuimbia Yahwe kwa kuwa ameniganga kwa ukarimu kabisa.

# 14

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi. 1 Mpumbavu husema moyoni mwake,
“Hakuna Mungu.” Wamepotoka nakufanya uovu haramu; hakuna hata mmoja
atendaye dhambi. 2 Yahwe anatazama chini kwa wanadamu kutoka mbinguni
aone kama kuna yeyote anayeelewa, amtafutaye Mungu. 3 Wote wamegeukia njia
nyingine. Kwa pamoja wamepotoka. Hakuna yeyote atendaye mema, hakuna, hata
mmoja. 4 Je, hawajui lolote, wale wafanyao uovu, wale wanao kula watu wangu
kama vile wanakula mkate, lakini hao hawamuiti Yahwe? 5 Wao wana tetemeka
kwa hofu. Kwa kuwa Mungu yuko pamoja na kusanyiko la wenye haki! 6 Ninyi
mnataka kumfedhehesha mtu maskini japo kuwa Yahwe ni kimbilio lake. 7 Oh,
kwamba wokovu wa Israeli ungetokea Sayuni! Wakati Yahwe akiwarudisha watu
wake kutoka utumwani, ndipo Yakobo atashangilia na Israeli itakuwa na furaha!

# 15

1 Zaburi ya Daudi. Yahwe, ni nani atabaki hemani mwako? Ni nani atakaye ishi
kwenye mlima wako mtakatifu? 2 Yeyote anaye tembea bila lawama, yeye hufanya
kilicho haki na huongea ukweli kutoka moyoni mwake. 3 Yeye huwa hakashfu kwa
ulimi wake, hawadhuru wengine, na hamtusi jirani yake. 4 Mtu asiye na maana
hudharauliwa machoni pake, bali yeye huwaheshimu wale wanao mhofu Yahwe.
Yeye huapa kwa hasara yake mwenyewe na habadilishi ahadi yake. 5 Yeye habadilishi
nia yake aazimapo fedha. Yeye hachukui rushwa ili kumshuhudia kinyume asiye na
hatia. Yeye afanyanyaye mbambo haya hatatikisika kamwe.

# 16

Zaburi ya Daudi. 1 Unilinde, Mungu, kwa kuwa nakimbilia kwako kwa ajili ya
usalama. 2 Nami ninasema kwa Yahwe, “Wewe ni Bwana wangu; wema wangu
ni bure pasipo wewe. 3 Kama kwa watakatifu walioko duniani, ndio walio bora;
furaha yangu yote iko kwao. 4 Taabu yao itaongezeka, wale watafutao miungu
mingine. Sitamimina sadaka ya damu kwa miungu yao. Wala kuyainua majina yao
kwa midomo yao. 5 Yahwe, wewe ni sehemu ya chaguo langu na kikombe changu.
Unaishikilia kesho yangu. 6 Mistari iliyo pimwa imelelazwa mahari pa kufurahisha
kwa ajili yangu; hakika urithi ufurahishao ni wangu. 7 Nitakubariki Yahwe, wewe
unishauliye; hata wakati wa usiku akili zangu za nielekeza. 8 Nimemuweka Yahwe
mbele yangu kila wakati, ili nisitikisike kutoka mkono wake wa kuume. 9 Kwa
hiyo moyo wangu unafuraha, utukufu wangu washangilia. Hakika nitaishi katika
usalama. 10 Kwa kuwa hautaiacha roho yangu kuzimuni. Wewe hautamuacha
mwaminifu wako kuliona shimo. 11 Wewe hunifundisha njia ya maisha; furaha tele
inakaa katika uwepo wako; furaha inakaa katika mkono wako wa kuume milele!”

# 17

1 Maombi ya Daudi. Sikia ombi langu kwa ajili ya haki, Yawhe; uusikilize mwito
wangu wa msaada. Uyasikilize maombi yangu yatokayo katika midomo isiyo na
udanganyifu. 2 Uthibitisho wangu na uje kutoka uweponi mwako; macho yako na
yaone kile kilicho sahihi! 3 Kama utaujaribu moyo wangu, kama utakuja kwangu
wakati wa usiku, wewe utanitakasa na hautapata mipango yeyote ya uovu; mdomo
wangu hautavunja sheria. 4 Kama kwa matendo ya binadamu, ni katika neno la
midomo yako ya kuwa nimejiepusha na njia za wahalifu. 5 Mwenendo wangu
umeshikila kwa umakini mwenendo wako; miguu yangu haija teleza. 6 Nakuita
wewe, kwa kuwa unanijibu, Mungu; geizia sikio lako kwangu na usikilize ninapo
ongea. 7 Onyesha uaminifu wa agano lako katika namna ya ajabu, wewe uokoaye kwa
mkono wa haki yako wale wanao kukimbilia wewe kutoka kwa adui zao. 8 Unilinde
kama mboni ya jicho lako; unifiche katika kivuli cha mbawa zako 9 kutoka katika
uwepo wa waovu ambao wananitusi, adui zangu wanizungukao. 10 Wao hawana
huruma kwa yeyote; midomo yao huongea kwa majivuno. 11 Wao wame zizunguka
hatua zangu. Wamekaza macho yao wanishambulie mpaka ardhini. 12 Wao ni kama
mfano wa hasira ya simba mawindoni. Ni kama simba kijana anapotokea mafichoni.
13 Inuka, Yahwe! Uwashambulie! Uwaangushe chini kwenye nyuso zao! Uyaokoe
maisha yangu kutokana na waovu kwa upanga wako! 14 Uniokoe kutoka kwa watu
hawa kwa mkono wako, Yahwe, kutoka kwa watu wa dunia hii ambao utajiri wao
ni maisha haya pekee! Wewe utayajaza matumbo ya wale uwathaminio na utajiri;
watakuwa na watoto wengi na wataacha utajiri wao kwa watoto wao. 15 Bali mimi,
nitauona uso wako katika haki; Nitashuhudiwa, pale nitakapo amka, na macho yako.

# 18

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi, mtumishi wa Yahwe, alipomwimbia
Yahwe maneno ya wimbo huu katika ile siku ambayo Yahwe alimuokoa kutoka
katika mkono wa adui zake wote na kutoka katika mkono wa Sauli. Yeye aliimba:
1 Nakupenda, Yahwe, nguvu yangu. 2 Yahwe ni mwamba wangu, ngome yangu,
yeye ambaye aniwekae kweye usalama; yeye ni Mungu wangu, mwamba wangu;
ninapata kimbilio kwake. Yeye ni ngao yangu, pembe ya wokovu wangu, na
ngome yangu. 3 Nitamuita Yahwe kwa sababu anastahili kusifiwa, na nitaokolewa
kutoka kwa adui zangu. 4 Kamba za mauti zilinizunguka, na mafuriko yakimbiayo
yalinielemea. 5 Kamba za kuzimu zilinizunguka; mitego ya mauti ilininasa. 6 dhiki

yangu nilimuita Yahwe; Niliita msaada kwa Mungu. Naye alisikia sauti yangu
kutoka hekaluni mwake; kuita kwangu msaada kulienda mpaka uweponi mwake; na
kuingia masikioni pake. 7 Kisha nchi ikatikisika na kutetemeka; misingi ya milima
pia ilitetemeka na kutikiswa kwa sababu Mungu alikuwa amekasirika. 8 Moshi
ulifuka kutoka kwenye pua zake, na moto mkali ulitokea mdomoni mwake. Makaa
yaliwashwa kwa moto huo. 9 Yeye alizifunua mbingu na alishuka chini, na giza nene
lilikuwa chini ya miguu yake. 10 Alipanda kwenye kerubi na akaruka; alinyiririka
kwenye mabawa ya upepo. 11 Yahwe alilifanya giza kuwa hema likimzunguka yeye,
wingu la mvua zito katika mbingu. 12 Mawe ya barafu na makaa ya moto yalianguka
kutoka katika mwangaza kabla yake. 13 Yahwe aliongea katika mbingu! Sauti ya
aliye juu ilisikika. 14 Yeye aliifyatua mishale yake na kuwatawanya adui zake; na radi
nyingi zenye mwanga alizitawanya katika maeneo tofauti tofauti. 15 Ndipo mifereji
ya maji ilitokea; misingi ya dunia ikadhihirishwa kwa mlio wa pigo lako, Yahwe
kwa sauti ya pumzi ya pua zako. 16 Yeye alishuka chini kutokea juu; akanishikilia
mimi! Akanivuta nje ya maji yafurikayo. 17 Aliniokoa kutoka kwa maadui zangu
wenye nguvu, kutoka kwa wale ambao walinichukia mimi, kwa kuwa walikuwa na
nguvu sana kuliko mimi. 18 Wao walikuja kinyume na mimi katika siku ile ya dhiki
yangu lakini Mungu alikuwa msaada wangu! 19 Yeye aliniweka huru katika eneo
pana la wazi; yeye aliniokoa kwa sababu alipenezwa nami. 20 Yahwe amenitunuku
mimi kwa sababu ya haki yangu; yeye amenirejesha mimi kwa sababu mikono
yangu ilikuwa misafi. 21 Kwa kuwa nimezitunza njia za Yahwe na sijafanya uovu
wa kumgeuka Mungu wangu. 22 Kwa kuwa amri zake zote za haki zimekuwa mbele
yangu; kama asemavyo, sijaenda kinyume nazo. 23 Pia nimekuwa sina hatia mbele
zake, na nimejiweka mwenyewe mbali na dhambi. 24 Hivyo Yahwe amenirejesha
kwa sababu ya haki yangu, na kwa sababu mikono yangu ilikuwa safi mbele ya
macho yake. 25 Kwa yeyote aliye mwaminifu, jionyeshe wenyewe kuwa mwaminifu;
kwa mtu asiye na lawama, jionyeshe mwenyewe kuwa usiye na lawama. 26 Kwa
yeyote aliye msafi, jionyeshe mwenyewe safi; bali ni mjanja kwa yeyote aliye geuzwa.
27 Kwa kuwa wewe huwaokoa watu walio taabishwa, lakini wewe huwashusha
chini wale wenye majivuno, yaani macho yaliyo jinua! 28 Kwa kuwa wewe huipa
mwanga taa yangu; Yahwe Mungu wangu hutia mwanga giza langu. 29 Kwa kuwa
kwa kupitia wewe ninaweza kuruka juu ya kiwazo kilichowekwa; kupitia Mungu
ninaweza kuruka juu ya ukuta. 30 Kama kwa Mungu: njia yake ni kamilifu. Neno la
Yahwe ni safi! Yeye ni ngao kwa yeyote anaye kimbilia katika yeye. 31 Kwa kuwa
nani ni Mungu ispokuwa Yahwe? Nani ndiye mwamba ispokuwa Mungu wetu?
32 Ni Mungu anitiaye nguvu ndani yangu kama vile mkanda, ambaye humweka mtu
mwenye lawama katika njia yake. 33 Yeye hunifanya miguu yangu kuwa myepesi
kama mbawala na kuniweka mahali pa juu! 34 Yeye hufunza viganja vyangu kwa
ajili ya vita na mikono yangu kupiga upinde wa shaba. 35 Wewe umenipa mimi
ngao ya wokovu. Mkono wako wa kuume umenisaidia, na neema yako imenifanya
kuwa mkubwa. 36 Wewe umetengeneza nafasi pana kwa ajili ya miguu yangu ili
miguu yangu isiteleze. 37 Ninawashawishi adui zangu na kuwakamata; nami sikurudi
nyuma mpaka walipo haribiwa. 38 Niliwashambulia hata hawakuweza kuamka; nao
wameangukia chini ya miguu yangu. 39 Kwa kuwa unanitia nguvu kama mshipi
kwa ajili ya vita; wewe unawaweka chini yangu wale ambao wanainuka kinyume
na mimi. 40 Wewe ulinipa visogo vya maadui zangu; niliwaagamiza wale walio
nichukia. 41 Wao waliita msaada lakini hakuna aliye wasaidia; walimuita Yahwe,
lakini hakuwaitikia. 42 Niliwapiga wao katika vipande vidogo vidogo kama vile vumbi
mbele ya upepo; niliwatupa nje kama udongo mtaani. 43 Wewe uliniokoa mimi

kutoka katika migogoro ya watu. wewe umenifanya kichwa juu ya mataifa. Watu
ambao sikuwahi kuwafahamu huntumikia. 44 Pindi tu waliposikia kuhusu mimi, wao
walinitii; wageni walilazimishwa kunisujudu. 45 Wageni walitoka kwenye ngome
yao wakitetemeka. 46 Yahwe anaishi; mwamba wangu usifiwe. Ainuliwe Mungu wa
wokovu wangu. 47 Yeye ni Mungu ambaye hutelekeza visasi kwa ajili yangu, ambaye
huwatiisha mataifa chini yangu. 48 Nimewekwa huru kutoka kwa adui zangu! wewe
uliniinua juu ya wale walioinuka kunyume na mimi! Wewe uliniokoa kutoka kwa
watu wenye vurugu. 49 Kwa hiyo nitakushukuru wewe, Yahwe, kati ya mataifa;
Nitaliimbia sifa jina lako! 50 Mungu hutoa ushindi mkuu kwa mfalme wake, na yeye
huonyesha uaminifu wa agano lake kwa mpakwa mafuta wake, kwa Daudi na ukoo
wake milele.

# 19

1 Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi. Mbingu za tangaza utukufu wa
Mungu, na mawingu hufanya kazi ya mikono yake ijulikane! 2 Siku hadi siku hotuba
hutokea; usiku hadi usiku hufunua maarifa. 3 Hakuna hotuba wala misemo; sauti zao
hazisikiki. 4 Bali maneno yao husambaa nje duniani kote, na hotuba zao hata mwisho
wa dunia. Yeye ametengeneza hema kwa ajili ya jua kati yao. 5 Jua liko kama mfano
wa bwana harusi akitokea chumbani kwake na kama mtu shujaa ambaye hushangila
pale anapokimbia mbio zake. 6 Jua huchomoza kutokea upeo wa macho na likikatisha
winguni kwenda jingine; hakuna chochote kinacho epuka joto lake. 7 Sheria ya Yahwe
ni kamilifu, huokoa roho; ushuhuda wa Yahwe ni wa kuaminika, ukifanya hekima
nyepesi. 8 Maelekezo ya Yahwe ni ya hakika, yakiufanya moyo kuwa na furaha;
amri ya Yahwe ni safi, ikileta mwanga kwenye macho yetu. 9 Hofu ya Yahwe ni safi,
inadumu milele; amri za haki ya Yahwe ni za kweli na zote ni za hakika! 10 Nazo zina
thamani kuliko dhahabu, nazo ni tamu kuliko asali na matone ya asali kutoka sega
la asali (sega la nyuki). 11 Ndiyo, kupitia hizo mtumishi wako anaonywa; na katika
kuziamini kuna thawabu. 12 Ni nani ambaye aweza kuyatambua makosa yake yote
mwenyewe? Unitakase makosa yaliyo fichika. 13 Pia umuepushe mtumishi wako na
dhambi za majivuno; usiziruhusu kunitawala. Ndipo nitakuwa mkamilifu, na mimi
sitakuwa na hatia ya makosa mengi. 14 Maneno ya midomo yangu na mawazo ya
moyo wangu nayakubalike machoni pako, ewe Yahwe, mwamba wangu na mkombozi
wangu.

# 20

1 Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi. Mungu akusaidie wakati wa shida;
na jina la Mungu wa Yakobo likulinde 2 na kutuma msaada kutoka mahali patakatifu
kwa ajili ya kukutegemeza wewe kutoka Sayuni. 3 Naye akumbuke sadaka yako yote
na kuipokea sadaka ya kuteketezwa. 4 Naye akujalie haja za moyo wako na kutimiza
mipango yako yote. 5 Ndipo tutakapo shangilia katika ushindi wako, na, katika jina
la Mungu wetu, tutapeperusha bendera. Yahwe naakupe maombi yako yote ya haki.
6 Sasa ninajua ya kuwa Yahwe atawaokoa wapakwa mafuta wake; yeye atamjibu yeye
kutoka katika mbingu takatifu kwa uweza wa mkono wake wa kuume ambao waweza
kumuokoa yeye. 7 Baadhi hamini katika magari na wengine katika farasi, lakini
sisi tumuita Yahwe Mungu wetu. 8 Wao watashushwa chini na kuanguka, bali sisi
tutainuka na kusimama wima! 9 Yahwe, umuokoe mfalme; utusaidie sisi tukuitapo.

# 21

1 Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi. Mfalme anashangilia katika uweza
wako, Yahwe! Ni kwa namna kuu anashangilia katika wokovu uliouleta! 2 Wewe
umempa yeye matamanio ya moyo wake na hauja mkatalia maombi midomo yake.

3 Kwa kuwa wewe unamletea baraka nyingi; wewe uliweka katika kichwa chake taji
ya dhahabu iliyo safi kabisa. 4 Yeye alikuomba wewe maisha; ukampatia maisha;
wewe ulimpatia maisha malefu milele na milele. 5 Yeye utukufu wake ni mkuu
kwa sababu ya ushindi wako; wewe umemuwekea mapambo na enzi. 6 Kwa kuwa
unampatia yeye baraka za kudumu; unamfurahisha kwa furaha ya uwepo wako.
7 Kwa kuwa Mfalme humwamini Yahwe; kwa kupitia uaminifu wa agano la aliye juu
zaidi yeye hataondolewa. 8 Mkono wako utawakamata adui zangu wote wote; mkono
wako wa kuume utawakamata wale wote wanao kuchukia. 9 Wakati wa hasira yako,
wewe utawachoma kama katika tanuru la moto. Yahwe atawamaliza wao katika
hasira yake, na moto utawateketeza upesi wao. 10 Wewe utawaangamiza watoto
wao duniani na ukoo wao kutoka katika mrorongo wa wanadamu. 11 Kwa kuwa
walikusudia kukufanyia mambo maovu wewe; wao walitunga njama ambayo kwayo
hawawezi kufanikiwa! 12 Kwa kuwa wewe utawarudisha nyuma; wewe utafyatua
upinde wako mbele yao. 13 Uninuliwe, Yahwe, katika uweza wako; tutaimba na kusifu
nguvu zako.

# 22

Kwa kiongozi wa muziki; "aina ya muziki wa deer." Zaburi ya Daudi. 1 Mungu
wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? Kwa nini uko mbali na wokovu wangu
na mbali na maneno yangu yenye uchungu? 2 Mungu wangu, ninalia mchana kutwa,
lakini haunijibu, na wakati wa usiku sinyamazi! 3 Bado wewe ni mtakatifu; wewe
umekaa kama mfalme pamoja na sifa za Israeli. 4 Mababu zetu walikuamini wewe,
na wewe uliwaokoa wao. 5 Walikulilia wewe nao waka okolewa. Wao walikuamini
wewe na hawakuvunjwa moyo. 6 Bali mimi ni funza na sio mtu, nisiye faa kwa
ubinadamu na hudharauliwa na watu. 7 Wale wote wanionao hunisuta; hunidhihaki;
hunitikisia vichwa vyao. 8 Wao husema, "Yeye anamwamini Yahwe; mwache Yahwe
amuokoe. Mwache amuokoe yeye, kwa kuwa yeye anampendeza sana Yeye." 9 Kwa
kuwa wewe ulinileta kutoka tumboni; wewe ulinifanya nikuamini wewe wakati
nikiwa nanyonya matiti ya mama yangu. 10 Nimekwisha tupwa kwako wewe tokea
tumboni; wewe ni Mungu wangu tangu nikiwa tumboni mwa mama yangu! 11 Usiwe
mbali na mimi, kwa kuwa shida ikaribu; hayupo hata mmoja wa kusaidia. 12 Maksai
wengi wananizunguka mimi; maksai wenye nguvu ya Bashan wananizunguka mimi.
13 Wao wanafungua midomo yao kwangu kama simba aungurumaye akirarua windo
lake. 14 Ninamwagwa nje kama maji, na mifupa yangu yote imeteguka. Moyo
wangu ni kama nta; nao unayeyuka ndani ya sehemu zangu za ndani. 15 Nguvu
zangu zimekaushwa kama kipande cha ufinyanzi; ulimi wangu unanata juu ya
mdomo wangu. Wewe umenilaza mimi katika vumbi la mauti. 16 Kwa maana mbwa
wamenizunguka; kundi la watu waovu limenizunguka; wamenitoboa mikono yangu
na miguu yangu. 17 Nami ninaweza kuihesabu mifupa yangu. Wao wananitazama
na kunishangaa. 18 Wao wanagawa mavazi yangu kati yao wenyewe, wanapiga kura
kwa ajili ya mavazi yangu. 19 Usiwe mbali, Yahwe; tafadhali harakisha kunisaidia
mimi, nguvu yangu! 20 Uiokoe roho yangu na upanga, maisha yangu mwenyewe na
makucha ya mbwa mwitu. 21 Uniokoe na mdomo wa simba; uniokoe na mapembe
ya ng'ombe wa porini. 22 Nami nitalitangaza jina lako kwa ndugu zangu; katikati
ya kusanyiko la watu nitakusifu wewe. 23 Ninyi mnao mwogopa Yahwe, msifuni
yeye! Ninyi nyote kizazi cha Yakobo, muheshimuni yeye! Simameni katika hofu yake,
ninyi nyote kizazi cha Israeli! 24 Kwa kuwa haja dharau au kuchukia mateso ya aliye
taabishwa; Yahwe hajamficha uso wake yeye; pindi wale walio taabishwa walipo
mlilia yeye, yeye alisikia. 25 Yahwe, katika kusanyiko la watu wako nitakusifu kwa
yale uliyo tenda; nami nitatimiza nadhiri zangu mbele ya wale wanao muhofu yeye.

26 Walio onewa watakula na kutosheka; wale ambao humtafuta Yahwe watamsifu
yeye. Mioyo yenu iishi milele. 27 Watu wote wa duniani watakumbuka na kumrudia
Yahwe; familia zote za mataifa watapiga magoti chini mbele yako. 28 Kwa kuwa
utawala ni wa Yahwe; yeye ni mtawala wa mataifa. 29 Watu wote wa duniani
waliofanikiwa wata sherekea na wata abudu; wale wote washukao katika mavumbi
watapiga magoti mbele zake, wale ambao hawawezi kulinda maisha yao wenyewe.
30 Kizazi kijacho kitamtumikia yeye; wao watakiambia kizazi kinachofuatia kuhusu
Bwana. 31 Wao watakuja na kuzungumza kuhusu haki yake; wao watawaambia watu
ambao bado hawaja zaliwa yale ambayo Yahwe ameyafanya!

# 23

Zaburi ya Daudi. 1 Yahwe ni mchungaji wangu; sita pungukiwa na kitu. 2 Yeye
hunilaza katika majani mabichi; huniongoza kando ya maji matulivu. 3 Yeye
huurejesha uhai wangu; huniongoza katika njia iliyo sahihi kwa ajili ya jina lake.
4 Hata ijapokuwa nikipita katika bonde la uvuli na giza nene, sitaogopa kudhurika
kwa kuwa wewe uko pamoja nami; fimbo yako na gongo lako vya nifariji. 5 Wewe
waandaa meza mbele yangu katika uwepo wa maadui zangu; umenipaka mafuta
kichwa changu na kikombe changu kinafurika. 6 Hakika wema na uaminifu wa
agano vitaniandama siku zote za maisha yangu; nami nitaishi katika nyumba ya
Yahwe milele!

# 24

Zaburi ya Daudi. 1 Nchi ni ya Yahwe, na vyote viijazavyo, dunia, na wote wakaao
ndani yake. 2 Kwa kuwa yeye aliianzisha juu ya bahari na kuiimarisha juu ya mito.
3 Ni nani atakaye panda mlima wa Yahwe? Ni nani atakaye simama patakatifu pake?
4 Yeye ambaye ana mikono misafi na moyo safi; ambaye hajauinua uongo, na haja
apa kiapo ili kudanganya. 5 Yeye atapokea baraka kutoka kwa Yahwe na haki kutoka
kwa Mungu wa wokovu wake. 6 Kizazi cha wale wamtafutao Mungu ni kama hiki,
wale ambao wanautafuta uso wa Mungu wa Yakobo. 7 Inueni vichwa vyenu, ninyi
malango; muinuliwe juu, milango ya milango ya kudumu, ili kwamba Mfalme wa
utukufu aweze kuingia! 8 Huyu Mfalme wa utukufu ni nani? Yahwe, mwenye nguvu
na uweza; Yahwe, mwenye uweza katika vita. 9 Inueni vichwa vyenu, ninyi malango;
muinuliwe juu, milango ya kudumu, ili kwamba Mfalme wa utukufu aweze kuingia!
10 Huyu Mfalme wa utukufu ni nani? Yahwe wa majeshi, yeye ni Mfalme wa utukufu.

# 25

Zaburi ya Daudi. 1 Kwako, Yahwe, nayainua maisha yangu! 2 Mungu wangu,
ninaamini katika wewe. Usiniache niaibishwe; usiwaache maadui zangu wafurahie
ushindi wao kwangu. 3 Asiaibishwe mtu yeyote anaye kutumaini bali waaibishwe
wale watendao hila bila sababu! 4 Unijulishe njia zako, Yahwe; unifundishe njia
zako. 5 Uniongoze kwenye kweli yako na unifundishe, kwa kuwa wewe ni Mungu
wa wokovu wangu; ninakutumainia wewe siku zote za maisha yangu. 6 Kumbuka,
Yahwe, matendo yako ya huruma na uaminifu wa agano lako; kwa kuwa vimekuwapo
siku zote. 7 Usizikumbuke dhambi za ujana wangu wala uasi wangu; Uniweke
akilini mwako pamoja na uaminifu wa agano kwa zababu ya uzuri wa wako,
Yahwe! 8 Yahwe ni mzuri na mwenye haki; kwa hiyo yeye huwafundisha njia
mwenye dhambi. 9 Yeye huwaelekeza wanyenyekevu kwa kile kilicho sahihi na yeye
huwafundisha wao njia yake. 10 Njia zote za Yahwe ni za upendo wa kudumu na
niaminifu kwa wote wanao tunza agano na maagizo ya amri zake. 11 Kwa ajili
ya jina lako, Yahwe, unisamehe dhambi zangu, kwa kuwa ni nyingi mno. 12 Ni

nani ambaye anamuogopa Yahwe? Bwana atamfundisha yeye katika njia ambayo
anapaswa kuichagua. 13 Maisha yake yataenenda katika uzuri; na uzao wake
utairithi nchi. 14 Urafiki wa Yahwe ni kwa ajili ya wale wanao mheshimu yeye,
naye hulifanya agano lake lijulikane kwao. 15 Siku zote macho yangu yanamtazama
Yahwe, kwa kuwa yeye ataifungua miguu yangu kwenye nyavu. 16 Unigeukie mimi
na unihurumie; kwa maana niko peke yangu na niliye matesoni. 17 Maumivu ya
moyo wangu yameongezeka; uniondoe katika dhiki hii! 18 Tazama mateso yangu na
taabu yangu; unisamehe dhambi zangu zote. 19 Ona maadui zangu, kwa maana ni
wengi; wananichukia kwa chuki ya kikatili. 20 Uyalinde maisha yangu na uniokoe;
usiniache niaibishwe, Kwa kuwa kwako nakimbilia usalama! 21 Uadilifu na unyofu
vinihifadhi, kwa kuwa nina kutumainia wewe. 22 Mungu, uiokoe Israeli, na shida
yake yote!

# 26

Zaburi ya Daudi. 1 Unihukumu mimi, Yahwe, kwa kuwa nimeenenda katika
uadilifu; nimeamini katika Yahwe bila kusita. 2 Unichunguze, Yahwe, na unijaribu;
uujaribu usafi wa sehemu zangu za ndani na moyoni mwangu! 3 Kwa maana
uaminifu wa agano lako uko mbele ya macho yangu, na mwenendo wangu ni katika
uaminifu wako. 4 Mimi sichangamani na watu waovu, wala sichangamani na watu
wanafiki. 5 Ninachukia waovu, na siishi na waovu. 6 Ninaosha mikono yangu
kounesha sina hatia, na kuikaribia madhabahu yako, Yahwe, 7 kuimba wimbo wa
sauti ya sifa na kutoa taarifa ya matendo yako yote ya ajabu. 8 Yahwe, ninaipenda
nyumba ninayoishi, mahali ambapo utukufu wako unaishi! 9 Usiniangamize pamoja
na wenye dhambi, au maisha yangu na watu wenye kiu ya kumwaga damu, 10 ambao
katika mikono yao kuna njama, na ambao mkono wa kuume umejaa rushwa.
11 Lakini kwangu mimi, nitaenenda katika uadilifu; uniokoe na unihurumie. 12 Miguu
yangu husimama sehemu salama; katika kusanyiko la watu nitambariki Yahwe!

# 27

Zaburi ya Daudi. 1 Yahwe ni nuru yangu na wokovu wangu; nimuogope nani?
Yahwe ni salama ya maisha yangu; ni mhofu nani? 2 Wakati waovu waliponijia
kunila mwili wangu, wapinzani wangu na adui zangu walijikwaa na wakaanguka.
3 Ingawa jeshi hujipanga kupigana na mimi, moyo wangu hautaogopa; japo vita vijapo
inuka kupigana nami hata hapo nitabaki kuwa jasiri. 4 Kitu kimoja nimekiomba kwa
Yahwe, nami nitakitafuta hicho: kwamba niweze kukaa katika nyumba ya Yahwe
siku zote za maisha yangu, kuutazama uzuri wa Yahwe na kutafakari hekaruni
mwake. 5 Kwa kuwa katika siku ya shida ataniificha nyumbani mwake; ataniificha
katika mfuniko wa hema lake. Yeye ataniinua juu ya mwamba! 6 Kisha kichwa
changu kitainuliwa juu ya maadui wote wanizungukao, nami nitatoa sadaka ya
furaha hemani mwake! Nitaimba na kutunga nyimbo kwa Yahwe! 7 Sikia, sauti
yangu nikuitapo, Yahwe! Unihurumie, na unijibu! 8 Moyo wangu huongea kuhusu
wewe, “Utafute uso wake!” Nami nautafuta uso wako, Yahwe! 9 Usiufiche uso wako
mbali na mimi; usinikasirikie mimi mtumishi wako! Wewe umekuwa msaada wangu;
usiniache wala kunitelekeza, Mungu wa wokovu wangu! 10 Hata kama baba yangu
na mama yangu wakiniacha, Yahwe utanitunza kwako. 11 Unifundishe njia yako,
Yahwe! Kwa sababu ya adui zangu uniongoze katika njia salama. 12 Usiwaache
adui zangu wanifanyie watamanivyo, kwa sababu mashahidi wa uongo wameinuka
kinyume namimi, nao wanapumua vurugu! 13 Kitu gani kingeweza kunitokea kama
nisingeamini kuwa nitauona uzuri wa Yahwe katika nchi ya walio hai? 14 Umngoje
Yahwe; uwe imara, na moyo wako uwe jasiri! Umngoje Yahwe!

# 28

Zaburi ya Daudi. Kwako, 1 Yahwe, ninalia; mwamba wangu, usinipuuze. Ikiwa haunijibu, nitaungana na wale waendao chini kaburini. 2 Sikia kilio cha kusihi kwangu pale niitapo msaada kutoka kwako, niinuapo mikono yangu mbele ya mahali patakatifu zaidi! 3 Usiniburute pamoja na waovu, wale wafanyao uovu, waongeao amani na majirani zao lakini mioyoni mwao mna uovu. 4 Uwape kulingana na sitahili ya matendo yao na uwalipe kulingana na madai ya maovu yao, uwalipe kwa ajili ya kazi ya mikono yao na uwape kile wanachostahili. 5 Kwa sababu hawayaelewi matendo ya Yahwe wala kazi ya mikono yake, atawakanyaga kanyaga chini na hata wajenga tena wao. 6 Abarikiwe Yahwe kwa sababu yeye amesikia sauti ya kusihi kwangu! 7 Yahwe ni nguvu yangu na ngao yangu; moyo wangu wa humwamini yeye, na ninasaidiwa. Kwa hiyo moyo wangu hufurahia sana, nami nitamsifu yeye kwa kuimba. 8 Yahwe ni nguvu ya watu wake, naye ni mkombozi salama wa wapakwa mafuta wake. 9 Uwaokoe watu wako na uwabariki warithi wako. Uwe mchungaji wao na uwabebe milele.

# 29

Zaburi ya Daudi. 1 Mpeni sifa Yahwe, enyi wana wa Mungu! Mpeni sifa Yahwe kwa ajili ya utukufu wake na nguvu. 2 Mpeni Yahwe utukufu ambao jina lake linastahili. Mpigieni magoti Yahwe katika mapambo ya utakatifu. 3 Sauti ya Yahwe imesikika zaidi ya maji; Mungu wa radi ya utukufu, radi yaYahwe i juu ya maji mengi. 4 Sauti ya Yahwe ina nguvu; sauti ya Yahwe ni kuu. 5 Sauti ya Yahwe huivunja mierezi; Yahwe huivunja vipande vipande mierezi ya Lebanon. 6 Yeye huifanya Lebanoni kuruka kama ndama wa ng'ombe na Sirioni kama mwana wa nyati. 7 Sauti ya Yahwe hutoa miale ya moto. 8 Sauti ya Yahwe hutetemesha Jangwa; Yahwe hutetemesha jangwa la Kadeshi. 9 Sauti ya Yahwe huufanya miti mikubwa kutikisika na huipukutisha misitu. Kila mmoja katika hekalu lake husema, “Utukufu!” 10 Yahwe hukaa kama mfalme juu ya mafuriko; Yahwe hukaa kama mfalme milele. 11 Yahwe huwatia nguvu watu wake; Yahwe huwa bariki watu wake na amani.

# 30

Zaburi; wimbo wakati wa kuweka wakifu hekalu. Zaburi ya Daudi. 1 Nitakutukuza wewe, Yahwe, kwa kuwa umeniinua na haujawaruhusu maadui zangu juu yangu. 2 Yahwe Mungu wangu, nilikulilia wewe kwa ajili ya msaada, nawe ukaniponya. 3 Yahwe, wewe umeitoa roho yangu kuzimuni; nawe umeniweka hai mbali na kaburi. 4 Mwimbieni sifa Yahwe, ninyi waaminifu wake! Mshukuruni Bwana mkumbukapo utakatifu wake. 5 Kwa kuwa hasira yake ni ya muda tu; bali neema yake yadumu milele. Kilio huja usiku, bali furaha huja asubuhi. 6 Kwa ujasiri nilisema, “Sitatikiswa kamwe.” 7 Yahwe, kwa neema yako uliniweka mimi kama mlima imara; lakini ulipouficha uso wako, nilisumbuka. 8 Nilikulilia wewe, Yahwe, na kuomba msaada kwa Bwana wangu! 9 Kuna faida gani katika kifo changu, kama nitaenda kaburini? Je, mavumbi yatakusifu wewe? Yatatangaza uaminifu wako? 10 Sikia, Yahwe, na unihurumie! Yahwe, uwe msaidizi wangu. 11 Wewe umegeuza kuomboleza kwangu kuwa kucheza; wewe umeyaondoa mavazi yangu ya magunia na kunivisha furaha. 12 Hivyo sasa utukufu wangu utakuimbia sifa wewe na hautanyamaza; Yahwe Mungu wangu, nitakushukuru wewe milele!

# 31

1 Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi. In wewe, Yahwe, nakimbilia usalama; usiniache niaibishwe. Katika haki yako uniokoe. 2 Unisikie; uniokoe haraka; uwe mwamba wangu wa usalama, ngome ya kuniokoa. 3 Kwa kuwa wewe ni mwamba

wangu na ngome yangu; kwa hiyo kwa ajili ya jina lako, uniongoze na unielekeze.
4 Unitoe katika mtego ambao wameuficha kwa ajili yangu, kwa kuwa wewe ni
usalama wangu. 5 Mikononi mwako naikabidhi roho yangu; nawe utaniokoa, Yahwe,
mwenye kuaminika. 6 Ninawachukia wale wanaotumikia miungu isiyo na maana,
bali ninaamini katika Yahwe. 7 Nitafurahi na kushangilia katika uaminifu wa agano
lako, kwa kuwa uliyaona mateso yangu; wewe uliijua dhiki ya moyo wangu. 8 Wewe
haujaniweka kwenye mkono wa maadui zangu. Nawe umeiweka miguu yangu
mahali pa wazi papana. 9 Uniurumie, Yahwe, kwa maana niko katika dhiki; macho
yangu yanafifia kwa huzuni pamoja na moyo wangu na mwili wangu. 10 Kwa kuwa
maisha yangu yamechoshwa kwa huzuni na miaka yangu kwa kuugua kwangu.
Nimekuwa dhaifu kwa sababu ya dhambi zangu, na mifupa yangu inachakaa. 11 Kwa
sababu ya maadui zangu wote, watu wananibeza; majirani zangu wanaishangaa hali
yangu, na wale wanao nifahamu wanashtuka. Wale wanionao mitaani hunikimbia.
12 Nimesahaulika kama mtu aliye kufa ambaye hakuna mtu anaye mfikiria. Niko
kama chungu kilicho pasuka. 13 Kwa maana nimesikia minong'ono ya wengi, habari
za kutisha kutoka pande zote kwa pamoja wamepanga njama kinyume na mimi. Wao
wanapanga njama ya kuniua. 14 Bali mimi ninakuamini wewe, Yahwe; Ninasema,
“Wewe ni Mungu wangu.” 15 Hatima yangu iko mikononi mwako. Uniokoe mikononi
mwa maadui zangu na wale wanao nifukuzia. 16 Nuru ya uso wako imuangazie
mtumishi wako; uniokoe katika uaminifu wa agano lako. 17 Usiniache niaibishwe,
Yahwe; kwa maana ninakuita wewe! Waovu waaibishwe! Na wanyamaze kimya
kuzimuni. 18 Na inyamazishwe midomo midanganyifu ambayo husema maneno
mabaya kuhusu watu wenye haki huku wakiwa na kiburi na dharau. 19 Uzuri wako ni
wa namna gani nao umeuhifadhii kwa ajili ya wale wanao kuheshimu sana, ambao
wewe huufanya kwa ajili ya wale ambao hukimbilia kwako kwa ajili ya usalama
mbele ya watoto wote wa wanadamu! 20 Katika makao ya uwepo wako, wewe
huwaficha mbali na njama za watu. Wewe huwaficha mahali salama na ndimi zenye
vurugu. 21 Atukuzwe Yahwe, kwa maana yeye alinionesha maajabu ya uaminifu wa
agano lake mahali nilipoishi. 22 Ingawa kwa haraka zangu nilisema, “Nimeondolewa
machoni pako,” bali wewe ulisikia kusihi kwangu nilipokulilia wewe. 23 Enyi wafuasi
waaminifu, mpendeni Yahwe, Yahwe huwalinda waaminifu, lakini huwalipa wakaidi
ipasavyo. 24 Iweni imara na jasiri, ninyi nyote mnao mwamini Mungu kuwasaidia.

## 32

1 Zaburi ya Daudi. Zaburi. Amebarikiwa mtu yule aliyesamehewa makosa
yake, ambaye dhambi zake zimesitiriwa. 2 Amebarikiwa mtu yule ambaye Yahwe
hamuhesabii hatia na ambaye rohoni mwake hamna udanganyifu. 3 Nilipokaa
kimya, mifupa yangu ilidhohofika huku nikiugua muda wote. 4 Mchana na usiku
mkono wako ulinielemea. nguvu zangu zilikauka wakati wa kiangazi. Selah 5 Ndipo
nilipotambua makosa yangu kwako, nami sifichi tena uovu wangu. Nilisema,
“Nitakiri makosa yangu kwa Yahwe,” nawe ulinisamehe hatia ya dhambi zangu.
Selah 6 Kwa sababu ya haya, wale wote ambao ni wa kimungu wanapaswa kukuomba
wakati wa shida kubwa. Nayo mafuriko yajapo, hayatawapata watu hao. 7 Wewe u
mahali pangu pa kujifichia, nawe utanilinda matatizoni. Wewe utanizunguka pamoja
na nyimbo zaushindi. Selah 8 Nitakuelekeza na kukufundisha katika njia upasayo
kuiendea. Nitakuelekeza huku macho yangu yakikutazama. 9 Msiwe kama farasi
au kama nyumbu, ambao hawana uelewa; ni kwa hatamu na lijamu tu unaweza
kuwapeleka popote utakapo wao waende. 10 Waovu wanahuzuni nyingi, bali
uaminifu wa agano la Yahwe utamzunguka yule anaye mwamini yeye. 11 Furahini

katika Yahwe, na mshangilie, ninyi wenye haki; pigeni kelele za shangwe, ninyi nyote wenye haki mioyoni mwenu.

## 33

1 Furahini katika Yahwe, ninyi wenye haki; kusifu kwa wenye haki kwa faa sana.
2 Mshukuruni Bwana kwa kinubi; mwimbieni sifa kwa kinubi chenye nyuzi kumi.
3 Mwimbieni yeye wimbo mpaya; pigeni kwa ustadi na muimbe kwa furaha. 4 Kwa
kuwa maneno ya Mungu ni ya hakika, na kila afanyacho ni haki. 5 Yeye hupenda
haki na kutenda kwa haki. Dunia imejaa uaminifu wa agano la Yahwe. 6 Kwa
neno la Yahwe mbingu ziliumbwa, na nyota zote ziliumbwa kwa pumzi ya mdomo
wake. 7 Yeye huyakusanya maji ya baharini kama rundo; naye huiweka bahari
katika ghala. 8 Basi ulimwengu wote umwogope Yahwe; wenyeji wote wa ulimwengu
wamuhofu yeye. 9 Kwa maana yeye alisema, na ikafanyika; aliamuru, na ikasimama
mahali pake. 10 Yahwe huvunja muungano wa mataifa; naye huishinda mipango ya
wanadamu. 11 Mipango ya Yahwe husimama milele, mipango ya moyo wake ni kwa
ajili ya vizazi vyote. 12 Limebarikiwa taifa ambalo Mungu wao ni Yahwe, watu ambao
yeye amewachagua kama warithi wake. 13 Yahwe anatazama kutoka mbinguni;
yeye huona watu wote. 14 Kutokea mahali ambapo yeye anaishi, huwatazama wote
waishio juu ya nchi. 15 Yeye anaye iumba mioyo yao na kuyaona matendo yao yote.
16 Hakuna mfalme anayeokolewa na jeshi kubwa; shujaa haokolewi na nguvu zake
nyingi. 17 Farasi sio salama kwa ajili ya ushindi; ijapokuwa nguvu zake ni nyingi,
hawezi kuokoa. 18 Tazama, macho ya Yahwe yako kwa wale wanao mhofu yeye,
wale wanao litumainia agano lake takatifu 19 kuwaokoa maisha yao na mauti na
kuwaweka hai wakati wa jaa. 20 Sisi tunamngoja Yahwe, yeye ni msaada wetu na
ngao yetu. 21 Mioyo yetu hufurahia ndani yake, kwa kuwa tunaamini katika jina
lake takatifu. 22 Yahwe, agano lako takatifu, liwe pamoja nasi tuwekapo tumaini letu
katika wewe.

## 34

Zaburi ya Daudi; wakati alipojifanya kuwa mwendawazimu mbele ya Abimeleki,
ambaye alimtoa yeye nje. 1 Nitamsifu Yahwe wakati wote, siku zote sifa zake zitakuwa
mdomoni mwangu. 2 Nitamsifu Yahwe! walio onewa wasikie na kufurahi. 3 Msifuni
Yahwe pamoja nami, kwa pamoja tuliinue jina lake. 4 Nilimuomba Yahwe msaada
naye akanijibu, akanipa ushindi juu ya hofu yangu yote. 5 Wale wanao mtazama
yeye wana furaha, na nyuso zao hazina aibu. 6 Huyu mtu aliye onewa alilia na
Yahwe akamsikia na kumuokoa kwenye matatizo yake yote. 7 Malaika wa Yahwe
huweka kambi wakiwazunguka wale wanao muogopa yeye na kuwaokoa. 8 Onjeni
muone Yahwe ni mzuri. Amebarikiwa mtu yule ambaye Yahwe ni kimbilio lake.
9 Muogopeni Yahwe, ninyi watu watakatifu wake. Hakuna kupungukikwa kwa wale
wanao mhofu yeye. 10 Simba wadogo wakati mwingine hukosa chakula na kuteseka
kwa njaa, bali wale wamtafutao Yahwe hawatapungukiwa chochote kilicho kizuri.
11 Njoni, wana, mnisikilize mimi. nitawafundisha ninyi hofu ya Yahwe. 12 Mtu nani
aliyepo ambaye anatamani maisha na anapenda kuwa na siku nyingi, ili kwamba
aweze kuona vizuri? 13 Hivyo uepushe ulimi wako na uovu na uilinde midomo yako
kuongea uongo. 14 Uache uovu na utende mema. Uitafute amani na kuiendea amani.
15 Macho ya Yahwe yako kwenye haki na masikio yake huelekea kulia kwao. 16 Uso
wa Yahwe uko kinyume na wale watendao uovu, kuikatilia mbali kumbukumbu yao
duniani. 17 Wenye haki hulia na Yahwe husikia na kuwaokoa kwenye matatizo yao
yote. 18 Yahwe yu karibu nao waliovunjika moyo, naye huwaokoa waliogandamizwa
rohoni. 19 Mateso ya wenye haki ni mengi, bali Yahwe huwaokoa nayo yote. 20 Yeye

huitunza mifupa yake yote, hakuna hata mmoja wao utavunjika. 21 Uovu utawauwa
waovu. Wale wachukiao haki watahukumiwa. 22 Yahwe huokoa maisha ya watumishi
wake. Hakuna atakaye hukumiwa hata mmoja atafutaye usalama katika yeye.

# 35

Zaburi ya Daudi. 1 Yahwe, uwashughulikie wale wanao nishughulikia mimi;
upigane nao wanao pigana nami. 2 Uikamate ngao yako ndogo na ngao kubwa; inuka
unisaidie. 3 Uutumie mkuki wako na shoka lako la vita kwa wale wanao nifukuzia;
uuambie moyo wangu, "Mimi ni wokovu wako." 4 Waaibishwe na kudharauliwa
wale wanaoutafuta uhai wangu. Warudishwe nyuma na wafedheheshwe wanao
panga kunidhuru. 5 Wao wawe makapi mbele ya upepo, malaika wakiwafutilia
mbali. 6 Njia yao na iwe giza na utelezi, malaika wa Yahwe wakiwafukuzia.
7 Wamenitegea mtego bila sababu; bila sababu wamechimba shimo kwa ajili ya uhai
wangu. 8 Uharibifu na uwapate wao kwa kushitukiza. Mtego ambao wameutega
na uwanase wao. Na wadumbukie humo, ili kwamba waangamizwe. 9 Bali mimi
nitakuwa nafuraha ndani ya Yahwe na ndani ya wokovu wake. 10 Mifupa yangu yote
itasema, "Yahwe, ni nani kama wewe, uokoaye walio onewa mkononi mwa walio
na nguvu kuwazidi wao na masikini na wahitaji mkononi mwa wale wanaojaribu
kuwaibia?" 11 Mashahidi wa uongo wamesimama; wananishitakia uongo. 12 Kwa ajili
ya wema wananilipa mabaya. Nina huzuni nyingi. 13 Lakini, walipokuwa akiugua,
nilivaa magunia; nilifunga kwa ajili yao huku kichwa changu kikiinamia kifuani
kwangu. 14 Nilienenda katika huzuni kana kwamba walikuwa ni ndugu zangu;
niliinama chini nikiomboleza kana kwamba ni kwa ajili ya mama yangu. 15 Bali
mimi nilipokuwa mashakani, walifurahi sana na kukutanika pamoja; walikutanika
pamoja kinyume na mimi, nami nilishangazwa nao. Walinirarua bila kuacha. 16 Kwa
dharau kabisa walinidhihaki; walinisagia meno yao. 17 Bwana, mpaka lini utaendelea
kutazama? uiokoe roho yangu na mashambulizi yao ya maagamizi uyaokoe maisha
yangu na simba. 18 Nami nitakushukuru wewe katika kusanyiko kubwa; nitakusifu
kati ya watu wengi. 19 Usiwaache maadui zangu wadanganyifu kufurahi juu yangu;
usiwaache waendelee na mipango yao ya uovu. 20 Kwa maana hawaongei amani,
bali wanabuni maneno ya uongo kwa wale wanaoishi kwa amani katika ardhi
yetu. 21 Midomo yao inapaza sauti ikinishtaki; wakisema, Aha, Aha, macho yetu
yameona." 22 Yahwe wewe umeona, usikae kimya; Bwana, usiwe mbali nami.
23 Inuka mwenyewe na usimame kunitetea; Mungu wangu na Bwana wangu, unitetee.
24 Kwa sabababu ya haki yako, Yahwe Mungu wangu, unitetee; usiwaache wafurahi
kwa ajili yangu. 25 Usiwaache waseme mioyoni mwao, "Aha, tumepata tulicho
kihitaji." Usiwaache waseme, tumemmeza." 26 Uwaaibishe na kuwa fendhehesha
wale wanaotaka kunidhuru. Wale wote wanao ni dhihaki wafunikwe kwa aibu na
kudharauliwa. 27 Nao wote wanao tamani kudhihirishwa kwangu washangilie na
wafurahi; siku zote waseme, "Usifiwe Yahwe, yeye ajifurahishaye katika mafanikio
ya mtumishi wake. 28 Kisha nitatangaza matendo yako ya haki na kukusifu wewe
wakati wote.

# 36

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi ya mtumishi wa Yahwe. 1 Dhambi
hunena kama unabii katika moyo wa mwovu; machoni mwake hamna hofu ya
Mungu. 2 Kwa maana yeye hujifariji mwenyewe, akifikiria kuwa dhambi zake
hazitagundulika na kuchukiwa. 3 Maneno yake ni yenye dhambi na udanganyifu;
hataki kuwa mwenye hekima na kutenda mema. 4 Alalapo kitandani, hupanga
namna ya kutenda dhambi; yeye hukaa nje kwenye nja ya uovu; yeye hakatai

uovu. 5 Uaminifu wa agano lako, Yahwe, unafika mbinguni; uaminifu wako unafika
mawinguni. 6 Haki yako ni kama milima ya Mungu; hukumu yako ni kama kina
kirefu. Yahwe, wewe huwahifadhi wote wanadamu na wanyama. 7 Ni jinsi gani
uaminifu wa aganao lako ni wa thamani, Mungu! Watu hukimbilia usalama chini ya
uvuli wa mbawa zako. 8 Nao watatoshelezwa tele na utajiri wa chakula nyumbani
mwako; utawafanya wanywe kutoka katika mto wa baraka zako za thamani. 9 Kwa
kuwa mna chemichemi ya uzima; na katika mwanga wako tutaiona nuru. 10 Uupanue
uaminifu wa agano lako kikamilifu kwa wale wanao kujua wewe, ulinzi wako
uwe juu ya wanyoofu wa moyo. 11 Usiuache mguu wa mwenye kiburi unisogelee.
Usiiache mkono wa mwovu unitoweshe. 12 Kule wafanyao maovu wameanguka;
wameharibiwa hawawezi kuinuka.

## 37

Zaburi ya Daudi. 1 Usikereshwe na wafanyao maovu; usiwaonee wivu wale
watendao yasiyo haki. 2 Kwa kuwa muda mfupi watakauka kama nyasi na kukauka
kama vile mimea ya kijani ikaukavyo wakati wa kiangazi. 3 Uwamini Mungu na
kufanya yaliyo mema; uishi katika nchi na uongezeke katika imani. 4 Kisha ufurahi
mwenyewe katika Yahwe, naye atakupa matamanio ya moyo wako. 5 Umkabidhi njia
zako Yahwe; uamini katika yeye, naye atatenda kwa niaba yako. 6 Yeye ataidhihilisha
haki yako kama mchana na usafi wako kama mwangaza wa mchana. 7 Uwe kumya
mbele za Yahwe na umsubiri yeye kwa uvumilivu. Usikasirike ikiwa kuna mtu
anafanikiwa kwa kile afanyacho, au afanyapo njama za uovu. 8 Usikasilile na
kugadhabika. Usiogope. Hii huleta matatizo tu. 9 Watendao maovu watafutiliwa
mbali, bali wale wamngojao Yahwe watairithi nchi. 10 Katika muda mfupi mtu
mwovu atatoweka; wewe utatazama mahali pake, wala hautamuona. 11 Lakini
wapole watairithi nchi nao watafurahia katika mafanikio makubwa. 12 Mtu mwovu
hupanga njama kinyume na mwenye haki na kumsagia meno. 13 Bwana humcheka,
kwa maana anaona siku yake inakuja. 14 Waovu wametoa nje panga zao na
wametayarisha pinde zao ili kuwaangamiza wanyonge na wahitaji, na kuwaua wenye
haki. 15 Panga zao zitawaua wenyewe, na pinde zao zitavunjika. 16 Ni bora kuwa
mwenye haki maskini kuliko tajiri mwenye mali nyingi. 17 Kwa maana mikono
ya watu waovu itavunjika, bali Yahwe huwasaidia watu wenye haki. 18 Yahwe
huwalinda watu wasio na lawama siku hadi siku, na urithi wao utakuwa wa milele.
19 Hawata aibika siku mbaya zijapo. Wakati wa njaa ufikapo wao watakuwa na
chakula cha kutosha. 20 Bali waovu wataangamia. Maadui wa Yahwe watakuwa kama
vile utukufu wa malisho; watamalizwa na kupotezwa katika moshi. 21 Mtu mwovu
hukopa lakini halipi, bali mtu mwenye haki ni mkarimu na hutoa. 22 Wale walio
barikiwa na Mungu watairithi nchi; wale aliowalaani watafutiliwa mbali. 23 Hatua za
mwanadamu zinaimarishwa na Yahwe, mtu ambaye njia zake zinakubalika machoni
pa Mungu. 24 Ajapojikwaa, hataanguka chini, kwa kuwa Yahwe anamshikilia kwa
mkono wake. 25 Nilikuwa kijana na sasa ni mzee; sijawahi kumuona mtu mwenye
haki ametelekezwa wala watoto wake kuombaomba mkate. 26 Wakati wote yeye
ni mkarimu na hukopesha, nao watoto wake hufanyika baraka. 27 Acha uovu na
ufanye yaliyo mema; ndipo utakapokuwa salama milele. 28 Kwa maana Yahwe
hupenda haki naye hawaachi wafuasi waaminifu. Wao hutunzwa milele, lakini
uzao wa waovu utafutiliwa mabli. 29 Wenye haki watairithi nchi na kuaa huko
milele. 30 Mdomo wa mwenye haki huongea hekima na huongeza haki. 31 Sheria
ya Mungu wake imo moyoni mwake; miguu yake haitelezi. 32 Mtu mwovu humvizia
mwenye haki na kutafuta kumuua. 33 Yahwe hatamuacha yeye kwenye mkono
wa mtu mwovu wala kumlaumu atakapohukumiwa. 34 Umngoje Yahwe na uishike

njia yake, naye atakuinua uimiliki nchi. Atakapo waondosha waovu wewe utaona.
35 Nimewaona waovu na mtu wa kutisha akienea kama mti wa kijani katika udongo
wa asili. 36 Lakini nilipopita tana mara nyingine, hakuwepo pale. nilimtafuta, lakini
sikumpata. 37 Uwachunguze watu waadilifu, na uwatambue wenye haki; kuna hatima
nzuri kwa ajili ya mtu wa amani. 38 Mwenye dhambi wataharibiwa kabisa; hatima ya
mtu mwovu ni kuondoshwa. 39 Wokovu wa haki unatoka kwa Yahwe; yeye huwalinda
wao nyakati za shida. 40 Yahwe huwasaidia na kuwaokoa. Yeye huwaokoa dhidi ya
watu waovu na kuwanusuru wao kwa sababu wao wamemkimbilia yeye kwa ajili ya
usalama.

# 38

Zaburi ya Daudi, kuirejeza katika kumbukumbu. 1 Yahwe, usinikemee katika hasira
yako; usiniadhibu katika ghadhabu yako. 2 Kwa kuwa mishale yako hunichoma, na
mkono wako huniangusha chini. 3 Mwili wangu wote unaumwa kwa sababu ya hasira
yako; kwa sababu ya dhambi zangu mifupa yangu haina afya. 4 Kwa maana maovu
yangu yamenielemea; yamekuwa mzigo mzito kwangu. 5 Vidonda vyangu vimeoza
na vinanuka kwa sababu ya upumbavu wa dhambi zangu. 6 Nimepindika na kuwa
mnyonge kila siku; ninaenenda katika maombolezo siku zote. 7 Kwa maana ndani
yangu, ninaungua; hakuna afya katika mwili wangu. 8 Nimedhohofika na kulemewa
sana; ninaugua kwa sababu ya dhiki yangu. 9 Bwana, wewe unaielewa shauku ya
ndani kabisa ya moyo wangu, na kuugua kwangu hakujifichika kwako. 10 Moyo
wangu unapwita pwita, nguvu zangu zinaniisha, macho yangu yanafifia. 11 Marafiki
na ndugu zangu wamenitenga kwa sababu ya hali; majirani zangu hukaa mbali
nami. 12 Wale wanaoutafuta uhai wangu hutega mitego kwa ajili yangu. Wao ambao
hutafuta kunidhuru huongea maneno ya uharibifu na husema maneno ya uongo siku
nzima. 13 Lakini, niko kama mtu kiziwi na sisikii lolote; niko kama mtu bubu ambaye
hasemi lolote. 14 Niko kama mtu asiye sikia na mbaye hawezi kujibu. 15 Hakika
ninakungoja wewe, Yahwe; wewe utanijibu, Bwana Mungu wangu. 16 Ninasema
hivi ili kwamba maadui zangu wasije wakafurahia juu yangu. Ikiwa mguu wangu
utateleza, watanifanyia mambo mabaya. 17 Kwa kuwa niko karibu mashakani, na
niko katika maumivu ya mara kwa mara. 18 Ninatubu makosa yangu; ninahuzunika
kwa dhambi zangu. 19 Lakini maadui zangu ni wengi; wale wanichukiao ni wengi.
20 Wao wananilipa mabaya kwa mema; wanavurumiza shutuma kwangu ingawa
nimefuata lililo jema. 21 Usinitelekeze, Yahwe, Mungu wangu, usikae mbali nami.
22 Njoo haraka unisaidie, Bwana, wokovu wangu.

# 39

Kwa kiongozi wa muziki, kwa ajili ya Jeduthun. Zaburi ya Daudi. 1 Niliamua,
“Nitakuwa mwangalifu kwa kile nisemacho ili kwamba nisitende dhambi kwa ulimi
wangu. Nitaufumba mdomo wangu niwapo uweponi mwa mtu mwovu.” 2 Nilikaa
kimya; Nilizuia maneno yangu hata kuongea lolote zuri, na maumivu yangu yalizidi
sana. 3 Moyo wangu ukawaka moto; nilipoyatafakari mambo haya, yaliniunguza
kama moto. Ndipo mwishowe niliongea. 4 Yahwe, unijulishe ni lini utakuwa mwisho
wa maisha yangu na kiwango cha siku zangu. Unioneshe jinsi maisha yangu yalivyo
mafupi. 5 Tazama, wewe umezifanya siku zangu kama upana wa kiganja changu
tu, sikuzangu za kuishi ni kama si kitu mbele zako. Hakika kila mtu ana pumzi
moja. Selah 6 Hakika kila mtu hutembea kama kivuli. Hakika kila mmoja hufanya
haraka kuhusu kukusaya utajiri ingawa hawajui ni nani atazipokea. 7 Sasa, Bwana,
ninasubiri kwa ajili ya nini? Wewe ni tumaini langu pekee. 8 Uniokoe na dhambi
zangu; usinifanye laumu ya wabumbavu. 9 Niko kimya na siwezi kufungua mdomo

wangu, kwa sababu ni wewe ndiwe umefanya hivyo. 10 Acha kunijeruhi; nimezidiwa
na pigo la mkono wako. 11 Wewe unapowaadhibu watu kwa ajili ya dhambi, huvila
kama nondo vitu vyao wavitamanivyo; hakika watu si kitu bali mvuke. Serah 12 Sikia
maombi yangu, Yahwe, na unisikilize; usikie kilio changu! Usiwe kiziwi kwangu, kwa
maana niko kama mgeni pamoja nawe, kimbilio langu la usalama kama mababu
zangu walivyokuwa. 13 Geuzia furaha yako kwangu ili kwamba niweze kutabasamu
kabla sijafa.

# 40

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi. 1 Nalimungoja Yahwe kwa uvumilivu;
alinisikia na kusika kilio changu. 2 Yeye akanitoa nje ya shimo la kutisha, nje ya
matope, naye aliiweka miguu yangu juu ya mwamba na kuzifanya hatua zangu
salama. 3 Yeye ameweka wimbo mpya mdomoni mwangu, sifa kwa Mungu.
Wengi watauona na kumheshimu yeye na kumwamini Yahwe. 4 Amebarikiwa
mtu yule ambaye humfanya Yahwe tumaini lake naye hathamini majivuno wala
wale wanaokengeuka kwa uongo. 5 Yahwe Mungu wangu, matendo ya ajabu
ambayo wewe umeyafanya, ni mengi, na mawazo yako yatuhusuyo sisi hayahesabiki;
Ikiwa ningetangaza na kuyazungumza kwao, ni mengi sana hayahesabiki. 6 Wewe
haufurahishwi katika sadaka au matoleo, bali wewe umeyafungua masikio yangu;
wala haukuhitaji sadaka ya kuteketeza au sadaka ya dhambi. 7 Ndipo nilisema mimi,
“Tazama, nimekuja; imeandikwa kuhusu mimi katika kitabu cha hati. 8 Ninafurahia
kuyafanya mapenzi yako, Mungu wangu; sheria zako ziko moyoni mwangu.” 9 Katika
kusanyiko kubwa nimetangaza habari njema ya haki yako; Yahwe, wewe unajua
sikuizuia midomo yangu. 10 Sikuficha haki yako moyoni mwangu; nimetangaza
uaminifu wako na wokovu wako; sijaficha uaminifu wa agano lako au uaminifu wako
kwenye kusanyiko kubwa. 11 Usiache kunitendea kwa rehema, Yahwe; Uaminifu
wa agano lako na uaminifu wako unihifadhi siku zote. 12 Mabaya yasiyo hesabika
yamenizunguka; Maovu yangu yamenipata nami siwezi kuona chochote; nayo ni
mengi kuliko nywele za kichwa changu, na moyo wangu umeniangusha. 13 Yahwe,
tafadhari uniokoe; njoo haraka unisaidie Yahwe. 14 Waaibike na wafedheheke
kabisa wanaufuatilia uhai wangu wauondoe. Warudishwe nyuma na wadharaulike,
wale wanaofurahia kuniumiza. 15 Waogopeshwe kwa sababu ya aibu yao, wale
waniambiao, “Aha, aha!” 16 Bali wale wote wakutafutao wafurahi na kushangilia
katika wewe; na kila mmoja apendaye wokovu wako aseme daima, “Asifiwe Yahwe.”
17 Mimi ni maskini na muhitaji; lakini Bwana hunifikiria. Wewe ni msaada wangu
nawe huja kuniokoa; usichelewe, Mungu wangu.

# 41

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi. 1 Amebarikiwa mtu yule amkumbukaye
mnyonge; katika siku ya taabu, Yahwe atamuokoa. 2 Yahwe atamuhifadhi na
kumuweka hai, naye atabarikiwa duniani; Yahwe hata mrudisha kwenye mapenzi
ya adui zake. 3 Awapo kwenye kitanda cha mateso Yahwe atamsaidia; nawe
utakifanya kitanda cha ugonjwa kuwa kitanda cha uponyaji. 4 Nami nilisema, “Yahwe
unihurumie! Uniponye, kwa maana nimekutenda dhambi wewe.” 5 Adui zangu
huongea maovu dhidi yangu, wakisema, 'Atakufa lini na jina lake lipotee?' 6 Adui
yangu ajapo kuniona, huongea mambo yasiyo na maana; moyo wake hukusanya
maafa yangu kwa ajili yake mwenyewe; na aondokapo kwangu, yeye huwaambia
watu wengine kuhusu hayo. 7 Wale wote wanaonichukia kwa pamoja hunon'gona
dhidi yangu; nao wanafarijika kwa ajili ya maumivu yangu. 8 Wakisema, “Gonjwa
baya limemshikilia yeye haswa; na sasa kuwa amelala kitandani, hatainuka kamwe.”

9 Kweli, hata rafiki yangu wa karibu, ambae nilimuamini, aliye kula mkate wangu,
ameinua kisigino chake dhidi yangu. 10 Bali wewe, Yahwe, unihurumie na uniinue
ili kwamba niwalipizie kisasi. 11 Na hivi nitajua kuwa unafurahishwa nami, kwa
kuwa adui yangu hatafurahia kunishinda. 12 Kwangu mimi, wewe unanisaidia katika
uadilifu wangu na utaniweka mbele ya uso wako milele. 13 Yahwe, Mungu wa Israeli
asifiwe milele na milele. Amen na Amen. Kitabu ya Pili

# 42

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya wana wa Korah 1 Kama ayala ayatamanivyo
maji ya mto. ndivyo hivyo ninakiu yako, Mungu. 2 Ninakiu yako Mungu, Mungu uliye
hai, ni lini nitaonekana mbele zako? 3 Machozi yangu yamekuwa ni chakula changu
mchana na usiku, wakati maadui zangu siku zote wanasema, “Yuko wapi Mungu
wako?” 4 Mambo haya niayakumbuka ninapoumimina roho yangu: nilipoenda na
umati wa watu na kuwaongoza kwenye nyumba ya Mungu kwa sauti ya shangwe
na kusifu, ni wengi tulisherekea. 5 Roho yangu, kwa nini unainama? Kwa nini
unahuzuni ndani yangu? Mtumaini Mungu, Kwa kuwa kwa mara nyingine nitamsifu
yeye ambaye ni wokovu wangu. 6 Mungu wangu, roho yangu imeinama ndani yangu,
kwa hiyo ninakukumbuka toka nchi ya Yordani, toka kwenye vilele vitatu vya mlima
Hermoni, na toka mlima wa Mizari. 7 Kina huita kina kwenye kelele za maporomoko
ya maji yako; mawimbi na mafuriko yako yote yako juu yangu. 8 Wakati wa mchana
Yahwe ataamuru uaminifu wa agano lake; na usiku wimbo wake utakuwa nami, ombi
kwa Mungu wa uhai wangu. 9 Nami nitasema kwa Mungu wangu, mwamba wangu,
“Kwa nini umenisahau? Kwa nini ninaenenda katika maombolezo kwa sababu ya
ukandamizaji wa adui yangu?” 10 Kama upanga mifupani pangu, maadui zangu
wananikemea, siku zote wakiniambia, “Yuko wapi Mungu wako?” 11 Roho yangu,
kwa nini umeinama chini? Kwa nini unahuzuni ndani yangu? Mtumaini Mungu
kwa kuwa nitamsifu tena yeye aliye wokovu wangu na Mungu wangu.

# 43

1 Mungu, uniletee haki, na unitetee dhidi ya taifa lisilo la kimungu. 2 Kwa kuwa
wewe ni Mungu wa nguvu zangu. Kwa nini umenikataa? Kwa nini ninaenenda katika
maombolezo kwa sababu ya ukandamizaji wa adui yangu? 3 Oh, tuma nuru yako na
kweli yako ziniongoze. Ziniletee mlima wako mtakatifu na makao yako. 4 Kisha
nitakwenda madhabahuni mwa Mungu, kwa Mungu wangu aliye furaha yangu kuu.
Nami nitakusifu wewe kwa kinubi, Ee Mungu, Mungu wangu. 5 Roho yangu, kwa
nini umeinama? Kwa nini unahuzuni ndani yangu? Kwa kuwa nitamsifu tena yeye
ambaye ni wokovu wangu na Mungu wangu.

# 44

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya mwana wa Korah..... 1 Mungu, tumesikia
kwa masikio yetu, baba zetu wametuambia kazi uliyofanya katika siku zao, siku
za kale. 2 Uliwafukuza mataifa kwa mkono wako, lakini ukawafanya watu wetu
kuishi humo; wewe uliwataabisha mataifa, lakini ukawaeneza watu wetu katika
nchi. 3 Kwa maana hawakupata umiliki wa nchi kwa upanga wao, wala mkono
wao wenyewe haukuwaokoa; bali mkono wako wakuume, mkono wako, na nuru
ya uso wako, na kwa sababu uliwaridhia. 4 Mungu, wewe ni Mfalme wangu, amuru
ushindi kwa ajili ya Yakobo. 5 Kwa uweza wako tutawaangusha chini maadui zetu;
kwa jina lako tutatembea juu yao, wale wanao inuka dhidi yetu. 6 Kwa maana
sitauamini upinde wangu, wala upanga wangu hautaniokoa. 7 Bali wewe ndeye
uliyetuokoa na adui zetu, na umewaaibisha wale watuchukiao. 8 Katika Mungu

tumefanywa kujivuna siku zote, nasi tutalishukuru jina lako milele. Selah 9 Lakini
sasa umetutupa na kutufedhehesha, na hauendi na majeshi yetu. 10 Umetufanya
kuwakimbia maadui zetu; na wale watuchukiao huchukua vitu vyetu vya thamani
kwa ajili yao wenyewe. 11 Umetufanya kama kondoo aliyeandaliwa kwa ajili ya
chakula na umetutawanya kati ya mataifa. 12 Wewe unawauza watu wako bure;
kwa kufanya hivyo haukupata faida. 13 Wewe umetufanya kukemewa na majirani
zetu, kuchekwa, na kudhihakiwa na wale wanao tuzunguka. 14 Umetufaya kituko
kati ya mataifa,..................................................... 15 Siku zote fedheha yangu iko mbele
yangu, na aibu ya uso wangu imenifunika 16 kwa sababu ya sauti yake iliyo kemea
na kutukana, kwa sababu ya adui na kisasi. 17 Yote haya yametupata sisi; bado
hatukukusahau wewe wala kulikosea agano lako. 18 Mioyo yetu haikukengeuka;
hatua zetu hazikuiacha njia yako. 19 Bali wewe umetuadhibu vikali katika mahali
pa mbweha na kutufunika na uvuli wa mauti. 20 Ikiwa tumelisahau jina la Mungu
wetu au kueneza mikono yetu kwa Mungu mgeni, 21 Mungu asingeligundua hili?
Kwa maana yeye anazijua siri za moyo. 22 Hakika, kwa ajili ya jina lako tutauawa
siku zote; tunahesabiwa kuwa kondoo kwa ajili ya kuchinjwa. 23 Bwana, amka, kwa
nini unalala? Inuka, usitutupe moja kwa moja. 24 Kwa nini unaficha uso wako
na kusahau mateso yetu na kukandamizwa kwetu? 25 Kwa maana tumeyeyushwa
kwenye mavumbi; miili yetu imeshikamana na ardhi. 26 Inuka utusaidie na utuokoe
kwa ajili ya uaminifu wa agano lako.

# 45

Kwa kiongozi wa muziki; seti kwenye Shoshanim. Zaburi ya wana wa Korah.......
Wimbo wa upendo. 1 Moyo wangu unafurika kwa neno zuri; nitasoma kwa sauti
maneno niliyo yaandika kuhusu mfalme; ulimi wangu ni kalamu ya mwandishi
mwenye ustadi. 2 Wewe u mzuri sana kuliko mwanadamu yeyote; neema
imemiminwa midomoni mwako; Kwa hiyo tunajua ya kuwa Mungu amekubariki
milele. 3 Weka upanga wako upande wako, wewe uliye mwenye nguvu, katika
utukufu wako na enzi yako. 4 Katika enzi yako enenda katika ushindi kwa sababu
ya uaminifu, upole, na haki; mkono wako wa kuume utakufundisha mambo ya
kutisha. 5 Mishale yako ni mkali; watu huanguka chini yako; mishale yako imo
ndani ya mioyo ya adui za mfalme. 6 Kiti chako cha enzi, Mungu ni cha milele na
milele; na fimbo ya haki ni fimbo ya utawala wako. 7 Umeipenda haki na kuchukia
uovu; kwa hiyo Mungu, Mungu wako, amekupaka mafuta ya furaha kuliko wenzako.
8 Mavazi yako yote hunukia manemane, udi, na mdalasini; kukoka katika majumba
ya pembe vyombo vya muziki wa nyuzi vimekufurahisha. 9 Binti za wafalme ni
kati ya wake zako waheshimiwa; na mkono wako wa kuume amesimama malikia
aliye vaa mavazi ya dhahabu ya Ofiri. 10 Sikiliza, mwanangu, tafakari na utege
sikio lako; uwasahahu watu wako na watu wa nyumba ya baba yako. 11 Hivyo
mfalme atautamani uzuri wako; yeye ni Bwana wako; umstahi. 12 Binti wa Tiro
atakuwepo akiwa na zawadi; matajiri kati wa watu watajipendekeza kwako. 13 Binti
mfalme katika jumba la kifahari ana utukufu wote; mavazi yake yametengenezwa
kwa dhahabu. 14 Naye ataongozwa kwa mfalme akiwa katika mavazi ya dhahabu;
mabikra, wenzake wanoumfuata, wataletwa kwako mafalme. 15 Wao wataongozwa
kwa furaha na shangwe; wataingia mahali pa mfalme. 16 Katika mahali pa baba
zako watoto wako watakuwepo, ambao wewe utawafanya kuwa wakuu katika nchi
yote. 17 Nami nitalifanya jina lako kukumbukwa katika uzao wote; kwa hiyo watu
watakushukuru milele na milele.

# 46

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya mwana wa Korah; seti kwenye Alamoth.
Wimbo. 1 Mungu kwetu ni kimbilio la usalama na nguvu, upatikanao tele wakati
wa mateso. 2 Hivyo hatutaogopa, hata kama dunia italazimika kubadilika, hata kama
milima italazimika kutetemeka na kuangukia kwenye mtima wa bahari, hata kama
maji yatavuma kwa kishindo kikuu, 3 hata kama milima itatetemeka kwa vurugu ya
maji. Selah 4 Kuna mto, mikondo yake huufanya mji wa Mungu kufurahi, mahali
patakatifu pa hema ya Aliye Juu. 5 Mungu yuko katikati yake; naye hatasogezwa;
Mungu atamsaidia, naye atafanya hivyo asubuhi na mapema. 6 Mataifa yalikasirika
na falme zikataharuki; yeye alipaza sauti yake, na nchi ikayeyuka. 7 Yahwe wa
majeshi yuko pamoja nasi; Mungu wa Yakobo ni kimbilio letu la usalama. Selah
8 Njoni, mtazame matendo ya Yahwe, uharibifu alioufanya juu ya nchi. 9 Anaisitisha
vita kwenye nchi; yeye anauvunja upinde na kuikata vipande vipande mishale;
anazichoma ngao. 10 Mkae kimya na mjue kuwa mimi ni Mungu; nitainuliwa juu
ya nchi. 11 Mungu wa majeshi yuko pamoja nasi; Mungu wa Yakobo ni kimbilio letu
la usalama. Serah

# 47

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya wana wa Korah. 1 Pigeni makofi, enyi watu
wote; mpigieni Mungu kelele za ushindi. 2 Kwa maana Yahwe Aliye Juu anatisha; ni
Mfalme mkuu dunia yote. 3 Yeye anawatiisha chini yetu na mataifa chini ya miguu
yetu. 4 Yeye huchagua urithi kwa ajili yetu, utukufu wa Yakobo ambaye alimpenda.
Serah 5 Mungu ameinuliwa juu kwa shangwe, Kwa mbiu ya shangwe Yahwe yu
juu. 6 Mwimbieni Mungu sifa, imbeni sifa; mwimbieni sifa Mfalme wetu, imbeni
sifa. 7 Kwa maana Mungu ni Mfalme duniani kote; mwimbieni mkiwa na uelewa.
8 Mungu anatawala mataifa yote; Mungu hukaa kwenye kiti cha enzi. 9 Wakuu wa
watu wamekusanyika pamoja kwa watu wa Mungu wa Ibrahimu; kwa kuwa ngao za
duniani ni za Mungu; yeye ameinuliwa juu sana.

# 48

Wimbo; zaburi ya wana wa Korah. 1 Yahwe ndiye aliye mkuu na mwenyekusifiwa
sana, katika mji wa Mungu wetu kwenye mlima wake mtakatifu. 2 Ni mzuri katika
mwinuko wake, furaha ya nchi yote, ni mlima Sayuni, kwenye upande wa kaskazini,
mji wa Mfalme mkuu. 3 Mungu amejifunua mwenyewe katika jumba lake la kifahari
kama kimbilio la usalama. 4 Maana, tazama, wafalme walikusanyika wenyewe; wote
pamoja walipita. 5 Nao waliuona, wakashangaa; walifadhaika, na wakaharakisha
kuondoka. 6 Pale pale tetemeko liliwashikilia, maumivu makali kama mwanamke
anaye zaa. 7 Kwa upepo wa mashariki wewe huivunja meli ya Tarshishi. 8 Kama
tulivyo sikia, vivyo hivyo tumeona katika mji wa Yahwe wa majeshi, katika mji wa
Mungu wetu; Mungu atautunza milele. Selah 9 Tumeutafakari uaminifu wa agano
lako, Mungu, katikati ya hekalu lako. 10 Kama lilivyo jina lako, Mungu, hivyo ndivyo
zilivyo sifa zako mpaka miisho ya dunia; mkono wako wa kuume umejaa haki.
11 Milma Sayuni na ufurahi, nao wana wa Yuda washangilie kwa sababu ya amri
ya haki yako. 12 Tembeeni katika Mlima Sayuni, muuzungukie mji, 13 mzitazame
kwa makini nguzo zake, na mtazame majumba yake ya kifahari ili kwamba muweze
kuwasimulia kizazi kijacho. 14 Kwa kuwa huyu Mungu ni Mungu wetu milele na
milele; naye atakuwa kiongozi wetu mpaka kufa.

# 49

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya wana wa Korah. 1 Sikieni hili, ninyi watu
wote; tegeni masikio, ninyi wenyeji wa dunia, 2 wote walio chini na walio juu, tajiri
na masikini wote pamoja. 3 Mdomo wangu utazungumza hekima na tafakari ya
moyo wangu itakuwa ya uelewa. 4 Nitaelekeza sikio langu kwenye mfano; nitaanza
mfano wangu kwa kinubi. 5 Kwa nini nilazimike kuziogopa siku za uovu, wakati
uovu umenizunguka kwenye visigino vyangu? 6 Kwa nini niwaogope wale wanao
amini katika mali zao na kujivuna kuhusu utajiri wao? 7 Ni hakika kuwa hakuna
yeyote atakaye muokoa ndugu yake au kumpa Mungu pesa kwa ajili yake, 8 Kwa
maana ukombozi wa uhai wa mtu ni gharama kubwa, na hakuna awezaye kulipa
kile tunacho daiwa. 9 Hakuna yeyote atakaye ishi milele ili mwili wake usioze.
10 Maana yeye ataona uozo. Watu wenye hekima hufa; wajinga pia huangamia na
kuacha mali zao kwa wengine. 11 Mawazo yao ya ndani ni kuwa familia zao zitaishi
milele, na mahali waishipo, kwa vizazi vyote; wanaita ardhi zao kwa majina yao
wenyewe. 12 Lakini mtu, kuwa na mali, haimaanishi atabaki hai; kama wanyama
walioangamia. 13 Hii ni hatma ya wafanyao ujinga baada ya kufa,................. 14 Kama
kondoo wamechaguliwa kwa ajili ya kuzimu na kifo kitakuwa mchungaji wao. Nao
watatawaliwa na wenye haki ifikapo asubuhi, na miili yao italiwa kuzimuni, wakiwa
hawana afasi ya kuishi kwa ajili yao. 15 Bali Mungu ataufufua uhai wangu kutoka
katika nguvu ya kuzimu; naye atanipokea. Selah 16 Msifadhaike mtu awapo tajiri,
utukufu wa nyumba yake uongezekapo. 17 Maana atakapo kufa hataondoka na
chochote; utukufu wake hautamfuata yeye. 18 Yeye huifurahisha nafsi yake awapo
hai na watu hukusifu wewe uishipo maisha yako mwenyewe- 19 naye atakwenda
kwenye ukoo wa baba zake naye kamwe hataiona nuru tena. 20 Yule ambaye ana
mali lakini hana ufahamu ni kama wanyama, ambao wataangamia.

# 50

Zaburi ya Asafu. 1 Mungu, Mwenye nguvu, Yahwe, amenena naye aliita nchi
toka mawio ya jua mpaka machweo yake. 2 Tokea Sayuni, Mungu ameangaza,
ukamilifu wa uzuri. 3 Mungu wetu huja naye hakai kimya; mbele yake moto hula,
na kuna dhoruba kubwa karibu naye. 4 Yeye huziita mbingu zilizo juu na nchi ili
kwamba aweze kuwahukumu watu wake: 5 Kwa pamoja kusanyikeni waaminifu
wangu kwangu, wale waliofanya nami agano kwa sadaka." 6 Mbingu zitatangaza
haki yake, kwa maana Mungu mwenyewe ndiye jaji. Serah 7 Sikilizeni, watu wangu,
nami nitazungumza; mimi ni Mungu, Mungu wenu. 8 Sitawakaripia ninyi kwa ajili ya
sadaka zenu; sadaka zenu za kuteketeza ziko nami siku zote. 9 Sitachukua ng'ombe
katika nyumba yenu, wala beberu katika mazizi yenu. 10 Kwa maana kila mnyama wa
msituni ni wangu, nao ng'ombe kwenye milima elfu ni wangu. 11 Ninawajua ndege
wa mlimani, na wanyama pori katika shamba ni wangu. 12 Kama ningekuwa na
njaa, nisingewaambia ninyi; maana ulimwengu ni wangu, na vyote vilivyomo. 13 Je!
sitakula nyama ya ngombe na kunywa damu ya mbuzi? 14 Mtoleeni Mungu sadaka
za shukurani, na mlipe viapo vyenu kwa Aliye Juu. 15 Mniite katika siku ya shida;
nami nitawaokoa 16 Lakini kwa waovu Mungu anasema, "Inawahusu nini kuitangaza
hali yangu, kwamba ninyi mmeliweka agano langu mdomoni mwenu, 17 wakati ninyi
mnayachukia maelekezo na mnayatupa maneno yangu? 18 Mumuanapo mwizi, ninyi
hukubaliana naye; ninyi na mnashirikiana na wale wafanyao uasherati. 19 Mwautoa
mdomo wenu kwa mabaya, huelezea udanganyifu. 20 Mnakaa na kuongea dhidi ya
ndugu yenu; na kukashfu mwana wa mama yenu. 21 Mmefanya mambo haya, lakini
nimekaa kimya, hivyo mlidhani kuwa ni mtu flani nilliye kama ninyi mlivyo. Lakini
nitawakaripia ninyi na kuwafunua, mbele ya macho yenu, mambo yote miliyofanya.

[22] Mlitilie maanani hili, ninyi mnao msahau Mungu, vinginevyo nitawakata ninyi
vipande vipande, na hatakuwepo yeyote wakuja kuwasaidia! [23] Yule atoaye sadaka
ya shukurani hunitukuza, na yeyote apangaye njia zake katika namna iliyo sahihi
nitamuonesha wokovu wa Mungu."

## 51

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi; wakati nabii Nathani amekuja kwake
baada ya kusikia kuwa alilala na Bathsheba. [1] Unirehemu, Mungu, kwa sababu
ya uaminifu wa agano lako; kwa ajili ya wingi wa matendo yako ya rehema,
uyafute makosa yangu. [2] Unioshe kabisa uovu wangu na unisafishe dhambi zangu.
[3] Kwa maana ninayajua makosa yangu, na dhambi yangu iko mbele yako siku zote.
[4] Dhidi yako, wewe pekee, nimetenda dhambi na kufanya uovu mbele ya macho
yako; uko sawa usemapo; wewe uko sahahi utoapo hukumu. [5] Tazama, nilizaliwa
katika uovu; pindi tu mama yangu aliponibeba mimba, nilikuwa katika dhambi.
Tazama, wewe unahitaji uaminifu ndani ya moyo wangu; [6] katika moyo wangu wewe
utanifanya niijue hekima. [7] Unisafishe kwa hisopo, nami nitakuwa safi; unioshe,
nami nitakuwa mweupe kuliko theluji. [8] Unifanye kusikia furaha na shangwe ili
kwamba mifupa ulioivunja ifurahi. [9] Uufiche uso wako mbali na dhambi zangu
na uyafute maovu yangu yote. [10] Uniumbie moyo safi, Mungu, na uifanye upya
roho ya haki ndani yangu. [11] Usiniondoe uweponi mwako, na usimuondoe roho
Mtakatifu ndani yangu. [12] Unirudishie furaha ya wokovu wako, na unihifadhi mimi
kwa roho ya utayari. [13] Ndipo nitawafundisha wakosaji jia zako, na wenye dhambi
watakugeukia wewe. [14] Unisamehe kwa ajili ya umwagaji damu, Mungu wa wokovu
wangu, nami nitapiga kelele za shangwe ya haki yako. [15] Ee Bwana, uifungue midomo
yangu, na mdomo wangu itazieleza sifa zako. [16] Kwa maana wewe haufurahishwi
katika sadaka, vinginevyo ningekutolea sadaka; wewe hauwi radhi katika sadaka ya
kuteketezwa. [17] Sadaka ya Mungu ni roho iliyovunjika. Wewe, Mungu hautadharau
moyo uliopondeka na kujutia. [18] Uitendee mema Sayuni katika nia yako nzuri;
uzijenge tena kuta za Yerusalem. [19] Kisha wewe utafurahia sadaka yenye haki, katika
sadaka za kuteketeza; ndipo watu wetu watatoa ng'ombe kwenye madhabahu yako.

## 52

Kwa kiongozi wa muziki. Maschil ya Daudi; wakati Doegi Mwedomi alipokuja
na kumwambia Sauli, na kumwambia yeye, "Daudi amekuja kwenye nyumba ya
Ahimeleki." [1] Kwa nini wewe unajivunia kufanya uovu, wewe mtu mwenye nguvu?
Uaminifu wa agano la Mungu huja kila siku. [2] Ulimi wako hupanga uharibifu
kama wembe mkali, na kufanya udanganyifu. [3] Wewe unapenda uovu kuliko
wema na udanganifu kuliko kuongea haki. Selah [4] Wewe hupenda maneno ambayo
huwaumiza wengine, wewe ulimi mdanganyifu. [5] Vivyo hivyo Mungu atakuadhibu
wewe milele; yeye atakuchukua na kukuondoa katika hema yako na kukung'oa
katika ardhi ya uhai. Selah [6] Wenye haki pia wataona na kuogopa; watamcheka
na kusema, [7] "Tazama, huyu ni mtu ambaye hakumfanya Mungu kuwa kimbilio
lake la usalama, bali aliamini katika wingi wa mali zake, naye alikuwa na nguvu
alipowaharibu wengine." [8] Lakini kwangu mimi, niko kama mti bora wa mzeituni
katika nyumba ya Mungu; Nami nitaamini uaminifu wa agano la Mungu milele na
milele. [9] Nitakushukuru wewe daima kwa uliyo tenda. Nitalisubiri jina lako, kwa
sababu ni zuri, uweponi mwa wantu wako wa kimungu.

# 53

Kwa kiongozi wa muziki; seti kwenye Mahalath. Maschil ya Daudi. [1] Mpumbavu
husema moyoni mwake, "Hakuna Mungu." Wamepotoka na kufanya machukizo;
hakuna mmoja atendaye mema. [2] Toka mbinguni Mungu hutazama chini kwa
wanadamu kuona kama kuna yeyote mweye akili, amtafutaye yeye. [3] Wote
wamekengeuka. Kwa pamoja wamepotoka. Hakuna atendaye mema, hata mmoja.
[4] Je, wale wanao fanya uovu hawana uelewa - wale walao watu wangu kana
kwamba wanakula mkate na hawamuiti Mungu? [5] Wao walikuwa katika hofu kuu,
ingawa hakuna sababu ya kuogopa ilikuwepo hapo; maana Mungu ataitawanya
mifupa ya yeyote atakaye kusanyika dhidi yako; watu kama hao wataaibishwa kwa
sababu Mungu amewakataa wao. [6] Oh, kwamba wokovu wa Israel ungepatikana
Sayuni! Wakati Mungu atakapowaleta watu wake kutoka kifungoni, ndipo Yakobo
atashangilia na Israeli itafurahi!

# 54

Kwa kiongozi wa muziki; kwenye vyombo vya nyuzi. Maschil ya Daudi; wakati
Ziphites alipokuja na kumwambia Sauli, "Hivi Daudi hakujificha pamoja nasi?"
[1] Uniokoe, Mungu, kwa jina lako, na kwa nguvu zako unihukumu. [2] Usikie maombi
yangu, Mungu; uyategee sikio maneno ya mdomo wangu. [3] Kwa maana wageni
wameinuka dhidi yangu, na watu wasio na huruma wanaitafuta roho yangu; nao
hawakumuweka Mungu mbele yao. Selah [4] Tazama, Mungu ni msaidizi wangu;
Bwana ndiye anisaidiaye. [5] Naye atawalipizia uovu maadui zangu; katika uaminifu
wako, uwaharibu! [6] Nitakutolea dhabihu kwa moyo mkunjufu; nitalishukuru jina
lako, Yahwe, kwa maana ni jema. [7] Kwa kuwa yeye ameniokoa katika kila shida;
macho yangu yamewatazama adui zangu yakiwa na ushindi.

# 55

Kwa kiongozi wa muziki; kwenye vyombo vya nyuzi. Maschili ya Daudi. [1] Uyategee
sikio maombi yangu, Mungu; nawe usijifiche mbali na kusihi kwangu. [2] Unitazame
kwa makini na unijibu; Sina pumziko katika shida zangu [3] kwa sababu ya sauti ya
adui zangu, kwa sababu ya ukandamizaji wa waovu; maana wananiletea matatizo
na kunitesa wakiwa na hasira. [4] Moyo wangu wasumbuka ndani yangu, na hofu
ya kifo imeniangukia. [5] Uwoga na kutetemeka kumenijia, nayo hofu imenielemea.
[6] Nikasema, "Oh, kama tu ningekuwa na mabawa kama njiwa! Ningelipaa mbali na
kupata pumziko. [7] Tazama, ningeenda mbali; ningekaa jangwani. Selah [8] Ningefanya
haraka kuja mafichoni mwako kuzikimbia dhoruba na tufani." [9] Uwaangamize,
Bwana, vuruga lugha zao! Kwa maana nimeona vurugu na ugomvi katika mji.
[10] Mchana na usiku wao huenda kwenye kuta zake; uchafu na ufisadi uko katikati
yake. [11] Uovu uko katikati yake; ukandamizaji na uongo hauiachi mitaa yake.
[12] Kwa maana hakuwa adui aliye nikemea, hivyo ningevumilia; wala ingekuwa ni
yule aliye nichukia aliyejiinua mwenyewe dhidi yagu, hivyo ningejificha asinione.
[13] Lakini ulikuwa wewe, mtu sawa na mimi, mwenzangu na rafiki yangu. [14] Tulikuwa
na ushirika mtamu pamoja; tuliingia katika nyumba ya Mungu tukiwa na umati
mkubwa. [15] Kifo na kiwapate ghafla; na washuke wakiwa hai kuzimuni, maana
ndiko waishiko waovu, hapo hapo kati yao. [16] Lakini kwangu mimi, nitamwita
Mungu, na Yahwe ataniokoa. [17] Wakati wa jioni, asubuhi na mchana ninalalamika
na kuomboleza; yeye atasikia sauti yangu. [18] Kwa usalama kabisa atayaokoa
maisha yangu na vita dhidi yangu, kwa maana wale waliopigana nami walikuwa
ni wengi. [19] Mungu, yule unayetawala milele, atawasikia na kuwaaibisha wao. Selah
Hawabadiliki, na hawamhofu Mungu. [20] Rafiki yangu ameinua mikono yake dhidi ya

wale waliokuwa na amani naye; Hakuheshimu agano alilokuwa nalo. 21 Mdomo wake
ulikuwa laini kama siagi, lakini moyo wake ulikuwa adui; maneno yake yalikuwa
laini kuliko mafuta, lakini yalikuwa ni panga zilizochomolewa. 22 Umtwike mizigo
yako Yahwe, naye atakusaidia; yeye hataruhusu mtu mwenye haki kuyumbayumba.
23 Bali wewe, Mungu, utawaleta waovu chini kwenye shimo la uharibifu; watu wenye
kiu ya kumwaga damu na waongo hawataishi hata nusu ya maisha kama wengine,
lakini mimi nitakuamini wewe.

# 56

Kwa kiongozi wa muziki; seti kwenye Jonath elem rehokim. Zaburi ya daudi.
Zaburi; wakati Wafilisti walipomchukua katika Gath. 1 Uwe na huruma nami,
Mungu, kwa maana watu wananishambulia! Muda wote wale wanao pigana nami
hunikaribia zaidi ili wanishambulie. 2 Adui zangu hunikanyaga muda wote; maana
ni wengi ambao kwa kiburi hupigana dhidi yangu. 3 Wakati nina woga, nitaweka
imani yangu katika wewe. 4 Katika Mungu, ambaye neno lake ninalisifu - nimeweka
imani yangu katika Mungu; sitaogopa; mtu wa kawaida atanifanya nini? 5 Muda
wote wanayageuza maneno yangu; mawazo yao yote yako kinyume na mimi kwa
ajili ya uovu. 6 Wanajikusanya kwa pamoja, wanajificha wenyewe, na kuzifuatilia
hatua zangu, wakisubiri kuniua. 7 Usiwaache waikimbie adhabu yako kwa ajili ya
uovu wao. Uwaangushe watu chini katika hasira yako, Mungu. 8 Wewe unahesabu
kutangatanga kwangu na kuweka machozi yangu kwenye chupa yako; je, hayako
kitabuni mwako? 9 Ndipo maadui zangu watakimbia katika siku ile nikuitapo wewe;
hili najua, kwamba Mungu yupo kwa ajili yangu. 10 Katika Mungu ambaye neno lake
ninalisifu, katika Yahwe ambaye neno lake ninalisifu, 11 katika Mungu ninaamini,
sitaogopa. Yeyote atanifanya nini? 12 Wajibu wa kutimiza viapo vyangu kwako uko
juu yangu, Mungu; nitatoa sadaka ya shukurani. 13 Kwa kuwa umeokoa uhai wangu
na mauti; umezuia miguu yangu isianguke, ili kwamba niweze kutembea mbele ya
Mungu katika nuru ya uhai.

# 57

Kwa kiongozi wa muziki; seti kwenye Al Tashheth. Zaburi ya Daudi. Zaburi;
wakati alipo mkimbia Sauli, pangoni. 1 Unihurumie, Mungu, unihurumie mimi,
kwa maana ninakukimbilia wewe mpaka matatizo haya yaishe. Ninakaa chini ya
mbawa za zako kwa ajili ya ulinzi mpaka huu uharibifu utakapoisha. 2 Nitakulilia
Mungu uliye hai, kwa Mungu, afanyaye mambo yote kwa ajili yangu. 3 Yeye atatuma
msaada kutoka mbinguni na kuniokoa, ana hasira na wale wanaonishambulia.
Selah Mungu atanitumia upendo wake mwema na uaminifu wake. 4 Uhai wangu
uko katikati ya simba; niko katikati ya wale walio tayari kunila. Niko katikati ya
watu ambao meno yao ni mikuki na mishale, na ambao ndimi zao ni kali kama
upanga. 5 Uinuliwe, Mungu, juu ya mbingu, utukufu wako uwe juu ya nchi yote.
6 Wao walisambaza nje wavu kwa ajili ya miguu yangu; nilikuwa na shida sana.
Walichimba shimo mbele yangu. Wao wenyewe wameangukia katikati ya shimo!
Selah 7 Moyo wangu umeponywa, Mungu, moyo wangu umeponywa, nitaimba, ndiyo,
nitaimba sifa. 8 Inuka, moyo wa thamani; inuka, kinanda na kinubi; nitaamka alfajiri.
9 Nitakushukuru wewe, Bwana, kati ya watu; Kati ya mataifa nitakuimbia sifa.
10 Maana upendo wako usiokwisha, huzifikia mbingu; na uaminifu wako mawinguni.
11 Uinuliwe, Mungu, juu ya mbingu; na utukufu wako uinuliwe juu ya nchi yote.

# 58

Kwa kiongiozi wa muziki; seti kwenye Al Tashheth. Zaburi ya Daudi. Zaburi. 1 Je,
ninyi watawala mnaongea haki? Mnahukumu kwa haki, ninyi watu? 2 Hapana,
mnafanya uovu mioyoni mwenu; munaeneza vurugu nchi yote kwa mikono yenu.
3 Waovu huenenda katika upotovu hata walipokuwa tumboni; wao wanaenenda
katika upotovu tangu kuzaliwa, wakiongea uongo. 4 Sumu yao ni kama sumu ya
nyoka; wako kama fira kiziwi azibaye masikio yake, 5 ambaye hasikilizi sauti ya
waganga, haijalishi ustadi walio nao. 6 Vunja meno yao midomoni mwao, Mungu;
uyatoe meno ya mwana simba, Yahwe. 7 Wayeyuke kama maporomoko ya maji;
wafyatuapo mishale yao, iwe kama haina ncha. 8 Wawe kama konokono ambaye
huyeyuka na kutoweka, kama mtoto aliye zaliwa kabla ya wakati ambaye hakuona
jua. 9 Kabla ya vyungu vyenu kupata joto la kuungua kwa miiba, yeye ataviondosha
kwa upepo mkali, miiba ya kijani yote na ile inayoungua. 10 Mwenye haki atafurahia
atakapoona kisasi cha Mungu; ataiosha miguu yake kwenye damu ya waovu, 11 hivyo
watu watasema, “Hakika kuna tuzo kwa ajili ya mtu wenye haki; hakika kuna Mungu
ahukumuye ulimwengu.”

# 59

Kwa kiongozi wa muziki; seti kwenye Tashheth. Zaburi ya Daudi. Zaburi; wakati
Sauli alituma, waliilinda nyumba ili kumuua Daudi. 1 Uniokoe dhidi ya adui zangu,
Mungu wangu; uniweke mahali pa juu mbali na wale wanaoinuka dhidi yangu.
2 Uniweke salama mbali na wafanyao kazi ya uovu, na uniokoe dhidi ya watu wenye
kiu ya damu. 3 Maana, tazama, wanasubiria uvamizini waniue. Wafanya maovu
wenye nguvu hujikusanya wenyewe pamoja dhidi yangu, lakini sio kwa sababu ya
makosa yangu au dhambi yangu, Yahwe. 4 Wao wanajiandaa kunikimbiza ingawa
sina kosa; amka unisaidie na unitazame. 5 Ewe, Yahwe Mungu wa majeshi, Mungu
wa Israeli, inika uwaadhibu mataifa yote; usiwe na huruma kwa mhalifu mwovu
yeyote. Selah 6 Wao wanarudi jioni, wanabweka kama mbwa na kuuzungukia mji.
7 Tazama, wanapiga kelele mbaya kwa midomo yao; panga ziko kwenye midomo
yao, maana wanasema, “Ni nani anaye tusikia?” 8 Lakini wewe, Yahwe, utawacheka;
wewe huwadhihaki mataifa yote. 9 Mungu, nguvu yangu, nitakuwa msikivu kwako;
wewe ni mnara wangu mrefu. 10 Mungu atakutana nami akiwa na uaminifu wa
agano lake; Mungu atanifanya nione shauku yangu juu ya adui zangu. 11 Usiwaue,
hivyo watu watasahau. Uwatawanye kwa nguvu zako na uwaangushe, Bwana ngao
yetu. 12 Kwa ajili ya dhambi za midomo yao na maneno ya midomo yao, wakamatwe
katika majivuno yao, na kwa laana na uongo ambao wao huelezea. 13 Uwamalize
katika gadhabu yako, uwamalize ili kwamba wasiwepo tena; wajue kuwa Mungu
anatawala katika Yakobo na mwisho wa nchi. Selah 14 Wakati wa jioni wao hurudi,
wakibweka kama mbwa wakiuzungukia mji. 15 Wanatangatanga wakitafuta chakula
na wanabweka kama mbwa kama hawajatosheka. 16 Lakini nitaimba kuhusu nguvu
zako, na asubuhi nitaimba kuhusu upendo wako imara! maana umekuwa mnara
wangu mrefu na kimbilio la usalama katika siku ya taabu. 17 Kwako, nguvu yangu,
nitaimba sifa; kwa kuwa Mungu ni mnara wangu mrefu, Mungu wa uaminifu wa
agano.

# 60

Kwa kiongozi wa muziki; seti kwenye Shushan Eduth. Zaburi ya Daudi, kwa ajili
ya kufundisha. Wakati alipopigana na Aram Naharaim pamoja na Aram Zobah, na
Joab walirudi na kuwaua Wendomi elfu kumi na mbili katika bonde la chumvi.
1 Mungu, wewe umetutupa; umeuvunja ulinzi wetu; wewe umekuwa hasirani;

utuwezeshe tena. 2 Wewe umeifanya nchi kutetemeka; umeipasua pasua; uiponye
nyufa zake, maana zinatikisika. 3 Wewe umewafanya watu wako kuona mambo
magumu; umetufanya tunywe mvinyo wenye kutufanya kupepesuka. 4 Kwa wale
wanao kuheshimu wewe, wewe umeweka bandera ionekane dhidi ya wale wabebao
upinde. Selah 5 Ili kwamba wale uwapendao waweze kuokolewa, utuokoe sisi kwa
mkono wako wa kuume na unijibu. 6 Mungu ameongea katika utakatifu wake,
“Nitashangilia; nitaigawanya Shekemu na kuligawa bonde la Sukothi. 7 Gileadi ni
yangu, na Manase ni yangu na Ephraimu pia ni kofia yangu ya chuma; Yuda ni fimbo
yangu ya kifalme. 8 Moabu ni bakuli langu la kunawia; juu ya Edomu nitatupa kiatu
changu; nitapiga kelele za ushindi kwa sababu ya Filisti.” 9 Ni nani atakaye nileta
kwenye mji imara? Ni nani ataniongoza kwenda Edomu? 10 Lakini wewe, Mungu, je,
haukutukataa? Wewe hauendi vitani pamoja na jeshi letu. 11 Utusaidie dhidi ya adui
yetu, maana msaada wa mwanadamu ni bure. 12 Kwa msaada wa Mungu tutashinda;
yeye atawakanyaga chini adui zetu.

# 61

Kwa kiongozi wa muziki; kwenye chombo cha nyuzi. Zaburi ya Daudi. 1 Sikia kulia
kwangu, shughulikia maombi yangu. 2 Kutokea mwisho wa nchi nitakuita wewe
wakati moyo wangu umeelemewa; uniongoze kwenye mwamba ulio juu kuliko mimi.
3 Maana wewe umekuwa kimbilio langu la usalama, nguzo imara dhidi ya adui.
4 Uniache niishi hemani mwako milele! Nipate kimbilio salama chini ya makazi
ya mbawa zako. Selah 5 Kwa kuwa wewe, Mungu, umesikia viapo vyangu, wewe
umenipa mimi urithi wa wale wanao liheshimu jina lako. 6 Wewe utaongeza maisha
ya mfalme; miaka yake itakuwa kama vizazi vingi. 7 Yeye atabakia mbele ya Mungu
milele. 8 Nitaliimbia sifa jina lako milele ili kwamba niweze kufanya viapo vyangu
kila siku.

# 62

Kwa kiongozi wa muziki; Baada ya namna ya Jeduthun. Zaburi ya Daudi. 1 Katika
ukimya ninamsubiri Mungu pekee; wokovu wangu watoka kwake. 2 Yeye pekee
ni mwamba wangu na wokovu wangu; yeye ni mnara wangu mrefu; sitasogezwa
kamwe. 3 Mpaka lini, ninyi nyote, mtamshambulia mtu, ili kwamba mumpindue
yeye kama ukuta ulio inama au kama fensi isiyo imara? 4 Wanashauliana naye ili tu
kumshusha chini kutoka kwenye nafasi yake heshimiwa; wao wanapenda kuongea
uongo; wanambariki yeye kwa midomo yao, lakini mioyoni mwao wana mlaani yeye.
Selah 5 Katika ukimya ninamsubiri Mungu pekee; kwa maana matumaini yangu yako
kwake. 6 Yeye pekee ni mwamba wangu na wokovu wangu; yeye ni mnara wangu
mrefu; sitasogezwa. 7 Na Mungu ni wokovu wangu na utukufu wangu; mwamba
wa nguvu yangu na kimbilio langu salama liko katika Mungu. 8 Mwaminini Mungu
wakati wote, ninyi watu; mimina moyo wako mbele zake; Mungu ni kimbilio salama
kwa ajili yetu. Selah 9 Hakika watu wenye msimamo mdogo ni ubatili, na watu
wenye msimamo mkubwa ni waongo; wao watakuwa wepesi kwenye mzani; uzito
wao pamoja ni wepesi kuliko kitu chochote. 10 Usiamini katika ukandamizaji au
wizi; usitumainie utajiri, maana hawatazaa matunda; usiuweke moyo wako kwenye
hivyo. 11 Mungu ameongea mara moja, mara mbili nimesikia hili: nguvu ni za
Mungu. 12 Pia kwako, Bwana, ni uaminifu wa agano, maana humlipa kila mtu kwa
kile alichokifanya.

# 63

Zaburi ya Daudi, wakati yeye alipokuwa katika jangwa la Yuda. 1 Mungu, wewe
ni Mungu wangu! Ninakutafuta wewe kwa bidii, moyo wangu unakiu yako, mwili
wangu unakutamani sana wewe, katika ukame na nchi iliyochoka mahali ambapo
hakuna maji. 2 Hivyo nimekutafuta wewe katika watu watakatifu kuona nguvu
zako na utukufu wako. 3 Kwa sababu uaminifu wa agano lako ni bora kuliko
uhai, midomo yangu itakusifu wewe. 4 Hivyo nitakutukuza wewe niwapo hai;
kwa jina lako nitainua mikono yangu juu. 5 Itakuwa kana kwamba nilikula mlo
wa mafuta na wenye kunona, kwa midomo ya furaha kinywa changu kitakusifu
wewe, 6 nikufikiripo kitandani mwangu na kukutafakari wewe wakati wa saa za
usiku. 7 Kwa maana umekuwa msaada wangu, na katika uvuli wa mbawa zako
ninafurahia. 8 Ninashikamana nawe; mkono wako wa kuume unanisaidia. 9 Lakini
wale watafutao kuuharibu uhai wangu wataenda chini kwenye sehemu ya chini
kabisa ya nchi; 10 watakabidhiwa kwa wale ambao mikono yao hutumia upanga,
nao watakuwa chakula cha mbweha. 11 Bali mfalme atashangilia katika Mungu;
yeyote anaye apa kupitia yeye atajivunia yeye, lakini vinywa ya wale wasemao uongo
watanyamazishwa.

# 64

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi. 1 Sikia sauti yangu, Mungu, usikilize
malalamiko yangu; unilinde dhidi ya hofu ya adui zangu. 2 Unifiche dhidi ya mipango
ya siri ya wafanyao maovu, unifiche dhidi ya watendao vurugu ya udhalimu. 3 Wao
wamenoa ndimi zao kama panga; wamelenga mishale yao, maneno machungu,
4 ili kwamba waweze kupiga kutoka mahali pa siri kwenda kwa mtu asiye na
hatia; wampige yeye kwa ghafla nao wasihofu lolote. 5 Wao wanahamasishana
wenyewe katika kupanga uovu; wanashauriana pamoja wao binafsi ili kuweka
mitego; nao husema, “Ni nani atakayetuona?” 6 Wanabuni mipango ya dhambi;
“Tumemaliza,” wanasema, “ni mpango makini.” Mawazo ya ndani na mioyo ya
watu ni ya kina. 7 Lakini Mungu atawapiga wao; ghafla watajeruhiwa kwa mishale
yake. 8 Watafanywa kuwa mashakani, kwa kuwa ndimi zao wenyewe ziko kinyume
nao; wote wawaonao watatikisa vichwa vyao. 9 Watu wote wataogopa na kutangaza
matendo ya Mungu. Kwa hekima watafikiria kuhusu kile yeye ametenda. 10 Wenye
haki watakuwa na furaha kuhusu Yahwe nao watakimbilia kwake; wote wenye haki
moyoni watajivuna katika yeye.

# 65

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi. Wimbo wa Daudi. 1 Kwako wewe, Mungu
katika Sayuni, sifa zetu za kungoja; viapo vyetu vitaletwa kwako. 2 Wewe usikiaye
maombi yetu, miili yote itakuja kwako. 3 Maovu yanatutawala sisi; kama yalivyo
makosa yetu, wewe utayasamehe. 4 Amebarikiwa mtu yule ambaye wewe huchagua
kumsogeza karibu yako ili kwamba aishi hekaluni mwako. Tutatoshelezwa kwa uzuri
wa nyumba yako, hekalu lako takatifu. 5 Katika haki wewe utatujibu sisi kwa kufanya
mambo ya ajabu, Mungu wa wokovu wetu; wewe ambaye ni ujasiri wa mwisho wote
wa nchi na wa wale walio mbali toka pande za bahari. 6 Kwa manaa ni wewe ndiye
uliyeifanya milima imara, wewe ambaye umefungwa mkanda wa uweza. 7 Ni wewe
unyamazishaye ngurumo za baharini; ngurumo za mawimbi yake, na vurugu za
watu. 8 Wale wanaoishi sehemu za mwisho kabisa wa nchi wanaogopa ushahidi
wa matendo yako; wewe hufanya mashariki na magharibi kushangilia. 9 Wewe huja
kuisaidia nchi; unainyeshea inchi; wewe unaiimarisha nchi vizuri; mto wa Mungu
umejaa maji; wewe humpa mwanadamu nafaka unapokuwa umekwisha iandaa nchi.

10 Wewe huyajaza matuta maji ya kutosha; wapasawazisha palipoinuka; wailainisha
nchi kwa manyunyu ya mvua; waibariki mimea kati yao. 11 Umeuvika mwaka taji ya
wema wako; mvumo wa mapito yako hudondosha unono katika nchi. 12 Majani ya
nyikani hudondosha umande, na vilima vimevikwa furaha. 13 Malisho yamevishwa
mifugo; mabonde pia yamefunikwa na nafaka; yanapiga kelele za shangwe, nayo
yanaimba.

# 66

Kwa kiongozi wa muziki. Wimbo, Zaburi. 1 Mpigieni Mungu kelele za shangwe,
nchi yote; 2 Imbeni utukufu wa jina lake; mzitukuze sifa zake. 3 Mwambieni Mugu,
"Matendo yako yanatisha kama nini! Kwa ukuu wa nguvu zako maadui zako
watajisalimisha kwako. 4 Nchi yote watakuabudu wewe na watakuimbia wewe;
wataliimbia jina lako." Selah 5 Njoni na mtazame kazi za Mungu; yeye anatisha katika
matendo yake awatendeayo wanadamu. 6 Aligeuza bahari kuwa nchi kavu; wao
walitembea kwa mguu juu ya mto; huko tulishangilia katika yeye. 7 Yeye anatawala
milele kwa nguvu zake; macho yake yanachunguza mataifa; waasi wasijivune. Selah
8 Mtukuzeni Mungu, enyi watu wa mataifa yote, sauti ya sifa zake isikike. 9 Yeye
atuwekaye hai, naye hairuhusu miguu yetu iteleze. 10 Kwa maana wewe, Mungu,
umetupima sisi, wewe umetupima kama inavyopimwa fedha. 11 Wewe ulituingiza
sisi kwenye wavu; uliweka mzigo mzito viunoni mwetu. 12 Wewe uliwafanya watu
wasafiri juu ya vichwa vyetu; tulipita motoni na majini, lakini ukatuleta mahali pa
wazi palipo salama. 13 Nitaingia nyumbani mwako nikiwa na sadaka ya kuteketezwa;
nitakulipa viapo vyangu 14 ambavyo midomo yangu iliahidi na kinywa changu
kiliongea nilipokuwa katika dhiki. 15 Nitakutolea sadaka ya kuteketezwa ya wanyama
wanene pamoja na harufu nzuri ya kondoo waume; Nitatoa ng'ombe na mbuzi.
Selah 16 Njoni, msikie, ninyi nyote mnao mwabudu Mungu, nami nitatangaza yale
yeye aliyoitendea roho yangu. 17 Nilimlilia kwa kinywa changu, naye alipendezwa
na ulimi wangu. 18 Kama ningelikuwa na dhambi ndani ya moyo wangu, Bwana
asingenisikiliza. 19 Lakini Mungu hakika amesikia; amesikia sautiya kuomba kwangu.
20 Atukuzwe Mungu, ambaye hakuyakataa maombi yangu wala kuweka uaminifu wa
agano lake mbali nami.

# 67

Kwa kiongozi wa muziki; kwenye vyombo vya nyuzi. zaburi, wimbo. 1 Mungu
atuhurumie sisi na kutubariki na kufanya nuru ya uso wake ituangazie Selah 2 ili
kwamba njia zako zijulikane nchi yote, wokovu wako kati ya mataifa yote. 3 Watu
wakusifu wewe, Mungu; watu wote wakusifu wewe. 4 Oh, mataifa wafurahi na
na kuimba kwa furaha, maana utawahukumu watu kwa haki na kuwaongoza
mataifa walioko duniani. 5 Watu wakushukuru wewe, Mungu; watu wote wakusifu
wewe. 6 Nchi imetoa mavuno yake na Mungu, Mungu wetu, ametubariki. 7 Mungu
ametubariki sisi, na miisho yote ya dunia itamuheshimu yeye.

# 68

Kwa kiongozi wa muziki; Zaburi ya Daudi, wimbo. 1 Mungu ainuke, maadui
zake watawanyike; pia wale wamchukiao wakimbie mbele zake. 2 Kama moshi
uondoshwavyo, hivyo uwaondoshe wao; kama nta iyeyukavo mbele ya moto, hivyo
waovu waangamizwe uweponi mwa Mungu. 3 Bali wenye haki wafurahi; washangilie
mbele za Mungu; washangilie na kufurahi. 4 Mwimbieni Mungu! Lisifuni jina lake!
Msifuni yule aendeshaye farasi kwenye tambarare ya bonde la Mto Yordani! Yahwe
ni jina lake! Shangilieni mbele zake! 5 Baba wa yatima, na mwamuzi wa wajane, ni

Mungu anayeishi mahali patakatifu. [6] Mungu huwaweka wakiwa katika familia; yeye
huwafungua wafungwa kwa kuimba bali waasi huishi katika ardhi kavu. [7] Mungu,
wewe ulipoenda mbele ya watu wako, ulipotembea kupitia jangwani, Selah [8] nchi
ilitetemeka; mbingu pia zilidondosha mvua katika uwepo wa Mungu, uweponi mwa
Mungu wakati alipokuja Sinai, uweponi mwa Mungu, Mungu wa Israeli. [9] Wewe,
Mungu, ulituma mvua nyingi; uliuimarisha urithi wako wakati ulipokuwa umechoka.
[10] Watu wako waliishi humo; Wewe, Mungu, uliutoa kwa wema wako kwa maskini.
[11] Bwana alitoa amri, na wale walio zitangaza walikuwa ni jeshi kuu. [12] Wafalme wa
majeshi wanakimbia, wanakimbia, na wanawake wakisubiri nyumbani kuvigawana
wao na familia zao vilivyotekwa nyara. [13] Njiwa walio vikwa fedha wakiwa na
mabawa ya njano ya dhahabu. Wakati baadhi ya watu wakikaa kati ya mifugo ya
kondoo, kwa nini umefanya haya? [14] Mwenyezi Mungu aliwatawanya Wafalme huko,
ilikuwa kama vile wakati wa theluji juu ya Mlima Salmoni. [15] Mlima mkubwa ni
milima wa mji wa Bashani; mlima mrefu ni mlima wa mji wa Bashani. [16] Ewe mlima
mrefu wa nchi, kwa nini unatazama kwa jicho la husuda, kwenye mlima ambao
Mungu ameutaka kwa ajili ya mahali ambapo yeye ataishi? Hakika, Yahwe ataishi
humo milele. [17] Magari ya Mungu ni ishirini elfu, maelfu juu ya maelfu; Bwana yu kati
yao katika mahari patakatifu, kama katika Sinai. [18] Wewe umepaa juu; uliwaongoza
mateka; umepokea zawadi kutoka kati ya watu, hata kutoka kwa wale waliopigana
dhidi yako, ili kwamba wewe, Yahwe Mungu, uweze kuishi huko. [19] Abarikiwe
Bwana, atubebeaye mizigo yetu, Mungu ambaye ni wokovu wetu. Selah [20] Mungu
wetu ni Mungu aokoaye; Yahwe Bwana ni yule awezaye kutuokoa sisi dhidi ya kifo.
[21] Lakini Bwana atapiga vichwa vya adui zake, mpaka kwenye ngozi ya kichwa
yenye nywele ya wale watembeao katika makosa dhidi yake. [22] Bwana alisema,
“Nitawarudisha adui zangu kutoka Bashani; nitawarudisha kutoka katika kina cha
bahari [23] ili kwamba upate kuwaangamiza adui zako, ukichovya mguu wako katika
damu, na ili kwamba ndimi za mbwa wako zipate mlo wao kutoka kwa adui zenu.”
[24] Mungu, wameona maandamano yako, maandamano ya Mungu wangu, Mfalme
wangu, kwenye mahali patakatifu. [25] Waimbaji walitangulia, walifuatiwa na wapiga
muziki, na katikati walikuwa wanawali wakicheza ngoma. [26] Mtukuzeni Mungu
katika kusanyiko; msifuni Yahwe, ninyi ukoo wa kweli wa Israeli. [27] Kuna Benjamini
kwanza, kabila dogo, kisha viongozi wa Yuda na watu wao, viongozi wa Zabuloni
na viongozi wa Naftali. [28] Mungu wenu, Israeli, ameamuru nguvu zenu; uzifunue
kwetu nguvu zako, Mungu, kama ulivyo zifunua wakati uliopita. [29] Uzifunue nguvu
zako kwetu toka katika hekalu la Yerusalemu, ambako wafalme huleta zawadi kwako.
[30] Pigeni kelele katika vita dhidi ya wanyama wa porini katika mianzi, dhidi ya watu,
lile kundi la mafahari na ndama. Wafedhehesheni na kuwalazimisha wawaletee
zawadi; watawanyeni watu wapendao kupigana vita. [31] Wakuu watatoka katika
Misri; Ethiopia itafanya haraka kuufikisha mkono wake kwa Mungu. [32] Mwimbieni
Mungu, enyi falme za nchi; Selah mwimbieni sifa Yahwe. [33] Kwake yeye apitaye juu
ya mbingu za mbingu, zilizokuwepo tangu zama za kale; tazama, yeye hupiga kelele
kwa nguvu [34] Tangazeni kuwa Mungu ni mwenye nguvu; enzi yake iko juu ya Israeli,
na nguvu zake ziko angani. [35] Mungu, mahali pako patakatifu panatisha; Mungu wa
Israeli, yeye huwapa watu wake nguvu na uweza. Atukuzwe Mungu.

## 69

Kwa kiongozi wa muziki; seti kwenye Shoshannim. Zaburi ya Daudi. [1] Uniokoe,
Mungu; maana maji yameweka uhai wangu hatarini. [2] Ninazama kwenye kina cha
matope, pasipo na hahari pa kusimama; nimekuja kwenye kina kirefu cha maji,
ambako mafuriko yananifunika. [3] Nimechoka sana kwa kulia kwangu; koo langu ni

kavu; macho yangu yanafifia wakati namngoja Mungu wangu. 4 Wale wanichukiao
bila sababu wako zaidi ya nywele za kichwa changu; wale ambao wangeweza
kuniua, wakiwa adui zangu kwa sababu zisizo sahihi, ni wengi mno; wanalazimisha
nirudishe kile ambacho sijaiba. 5 Mungu, wewe unaujua ujinga wangu, na dhambi
zangu hazifichiki kwako. 6 Usiwaache wale wanao kungoja wewe waaibishwe kwa
sababu yangu, Bwana Yahwe wa majeshi; usiwaache wale wanaokutafuta wewe
wadharauliwe kwa sababu yangu, Mungu wa Israeli. 7 Kwa ajili yako nimestahimili
lawama; aibu imeufunika uso wangu. 8 Nimekuwa mgeni kwa ndugu zangu, nisiye
fahamika wala kuaminika kwa watoto wa mama yangu. 9 Kwa maana bidii ya
nyumba yako imenila, na laumu zao wanao kulaumu wewe zimeniangukia mimi.
10 Wakati nilipolia na kutokula chakula, walinitukana. 11 Nilipoteneneza mavazi
ya gunia, nikawa kituko kwao. 12 Wale wakaao katika lango la mji huniseng'enya;
mimi ni wimbo wa walevi. 13 Lakini kwangu mimi, maombi yangu ni kwako, Yahwe,
wakati ambao wewe utayapokea; unijibu katika uaminifu wa wokovu wako. 14 Unitoe
matopeni, na usiniache nizame; uniondoe mbali na wale wanaonichukia na uniokoe
katika kina cha maji. 15 Usiache mafuliko ya maji yanielemee, wala kina kisinimeze.
Usiache mdomo wa shimo unimeze. 16 Unijibu, Yahwe, maana uaminifu wa agano
lako ni mwema; kwa maana rehema zako kwangu ni nyingi, unigeukie. 17 Usiufiche
uso wako mbali na mtumishi wako, maana niko katika dhiki; unijibu haraka. 18 Uje
kwangu na unikomboe. Kwa sababu ya adui zangu, uwe fidia yangu. 19 Wewe wajua
kulaumiwa kwangu, kuaibishwa kwangu, na kudharauliwa kwangu; wapinzani
wangu wote wako mbele yako. 20 Lawama imevunja moyo wangu; nimejawa na
huzuni kubwa; nilitafuta mtu wa kunihurumia, lakini hakuwepo; nilitafuta wafariji,
lakini sikupata. 21 Walinipa sumu kwa ajili ya chakula changu; katika kiu yangu
walinipa siki ninywe. 22 Meza yao mbele yao na iwe mtego; wafikiripo wako kwenye
usalama, iwe kitanzi. 23 Macho yao na yatiwe giza ili kwamba wasiweze kuona;
uvifanye viuno vyao kutetemeka daima. 24 Wamwagie gadhabu yako, ukali wa hasira
yako uwafikie wao. 25 Sehemu yao na iwe ukiwa; mtu yeyote asiishi katika hema
yao. 26 Kwa kuwa walimtesa yule uliyempa adhabu. Mara kwa mara walihesabu
maumivu ya wale walioumizwa. 27 Wakiwashtaki kuwa wamefanya uovu juu ya
uovu; usiwaache waje kwenye ushindi wa haki yako. 28 Uwafute kwenye Kitabu
cha Uzima na wasiandikwe pamoja na wenyehaki. 29 Lakini mimi ni maskini na
mwenye huzuni; uruhusu wokovu wako, Mungu, uniweke juu sana. 30 Nitalisifu jina
la Mungu kwa wimbo na nitamtukuza yeye kwa shukrani. 31 Nitamsifu Yahwe zaidi
kuliko ng'ombe au ndama aliye na mapembe na kwato. 32 Wanyenyekevu wameona
na kufurahi; ninyi mnao matafuta Mungu, mioyo yenu itiwe nguvu. 33 Maana Yahwe
husikia wenye uhitaji naye hawadharau wafungwa wake. 34 Mbingu na nchi zimsifu
yeye, bahari na vyote vitembeavyo majini. 35 Kwa maana Mungu ataiokoa Sayuni na
ataujenga tena mji wa Yuda; watu wataishi huko na kupata umiliki wao. 36 Ukoo wa
watumishi wake watairithi; nao walipendao jina lake wataishi humo.

# 70

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi; kuleta kumbukumbu. 1 Uniokoe,
Mungu! Yahwe, njoo haraka na unisaidie mimi. 2 Wale wajaribuo kuchukua uhai
wangu waaibishwe na kufedheheshwa; warudishwe nyuma na wasiheshimiwe, wale
wafurahiao katika maumivu yangu. 3 Warudishwe nyuma kwa sababu ya aibu yao,
wale wasemao, “Aha, aha.” 4 Wale wakutafutao wafurahi na kushangilia katika
wewe; wale waupendao wokovu wako siku zote waseme, “Mungu asifiwe.” 5 Lakini
mimi ni maskini na muhitaji; harakisha kwangu, Mungu; wewe ni msaada wangu
nawe huniokoa mimi. Yahwe, usichelewe.

# 71

[1] Katika wewe, Yahwe, napatakimbilio salama; usiniache niaibishwe. [2] Uniokoe na
kunifanya salama katika haki yako; geuzia sikio lako kwangu. [3] Uwe kwagu mwamba
kwa ajili ya kimbilio salama ambako naweza kwenda siku zote; wewe umeamuru
kuniokoa, kwa kuwa wewe ni mwamba wangu na ngome yangu. [4] Uniokoe mimi,
Mungu wangu, kutoka katika mkono wa asiye haki na katili. [5] Maana wewe ni
tumaini langu, Bwana Yahwe. Nimekuamini wewe siku zote tangu nilipokuwa
mtoto. [6] Nimekuwa nikisaidiwa na wewe tangu tumboni; wewe ndiye yule uliyenitoa
tumboni mwa mama yangu; sifa zangu zitakuhusu wewe siku zote. [7] Mimi ni
mfano bora kwa watu wangu; wewe ni kimbilio langu lenye nguvu. [8] Mama
yangu atajawa na sifa zako, siku zote akikuheshimu. [9] Usinitupe katika siku za
miaka ya uzee wangu; usiniache wakati nguvu zangu zitakapoisha. [10] Maana adui
zangu wanazungumza kuhusu mimi; wale wanao fatilia uhai wangu wanapanga
njama pamoja. [11] Wao husema, “Mungu amemuacha; mfuateni na mumchukue,
maana hakuna yeyote awezaye kumuokoa yeye.” [12] Mungu, usiwe mbali nami;
Mungu wangu, harakisha kunisaidia mimi. [13] Waaibishwe na kuharibiwa, wale
walio adui wa uhai wangu; wavishwe laumu na kudharauliwa, wale watafutao
kuniumiza. [14] Lakini nitakutumainia wewe siku zote na nitakusifu wewe zaidi na
zaidi. [15] Kinywa changu kitaongea kuhusu haki yako na wokovu wako mchana kutwa,
ingawa ziwezi kuzielewa maana ni nyingi mno. [16] Nitakuja na matendo yenye nguvu
ya Bwana Yahwe; nitataja haki yako, yako pekee. [17] Mungu, tangu ujana wangu
wewe umenifundisha; hata sasa ninatangaza matendo yako ya ajabu. [18] Hakika, hata
niwapo mzee na mvi kichwani, Mungu, usiniache mimi, kama ambavyo nimekuwa
nikitanga nguvu yako kwa vizazi vijavyo, na uweza wako kwa yeyote ajaye. [19] Pia
haki yako, Mungu, iko juu sana; wewe ambaye umefanya mambo makuu, Mungu, ni
nani aliye kama wewe? [20] Wewe ambaye umetuonesha sisi mateso mengi utatuhuisha
tena na utatupandisha tena juu kutoka kwenye kina cha nchi. [21] Uiongeze heshima
yangu; rudi tena na unifariji. [22] Nami pia nitakushukuru kwa kinubi kwa ajili ya
uaminifu wako, Mungu wangu; kwako nitaimba sifa kwa kinubi, Mtakatifu wa Israel.
[23] Midomo yangu itapiga kelele kwa sababu ya furaha wakati nikikuimbia sifa, hata
kwa roho yangu, ambayo wewe umeikomboa. [24] Ulimi wangu pia utaongea kuhusu
haki yangu mchana kutwa; maana wameaibishwa na kuvurugwa, wale waliotafuta
kuniumiza.

# 72

Zaburi ya Sulemani. [1] Mpe mfalme amri ya haki yako, Mungu, haki yako kwa
wana wa mfalme. [2] Naye awaamue watu wako kwa haki na maskini wako kwa haki
sawa. [3] Milima iwazalie watu amani; vilima navyo vizae haki. [4] Naye awahukumu
watu maskini; awaokoe watoto wa wahitaji na kuwavunja vipande vipande wenye
kuwatesa. [5] Na wakuheshimu wewe wakati wa jua, na kwa kipindi cha kudumu kwa
mwezi katika vizazi vyote. [6] Naye apate kuja kama mvua juu ya nyasi zilizokatwa,
kama manyuyu yanyunyizayo nchi. [7] Mwenye haki na astawi kwa wakati wake, na
amani iwepo kwa wingi mpaka mwezi utakapotoweka. [8] Na awe na mamlaka toka
bahari na bahari, na kutoka Mto hadi miisho ya dunia. [9] Na wote waishio jangwani
wainame mbele zake; adui zake na walambe mavumbi. [10] Wafalme wa Tashishi
na visiwa walete kodi; wafalme wa Sheba na Seba watoe zawadi. [11] Hakika wafalme
wote wamwinamie yeye; mataifa yote yamtumikie yeye. [12] Kwa kuwa yeye humsaidia
mhitaji na maskini asiye na msaidizi. [13] Yeye huwahurumia maskini na wahitaji, na
huokoa maisha ya wahitaji. [14] Huyaokoa maisha yao dhidi ya mateso na vurugu, na
damu yao ni ya thamani machoni pake. [15] Naye apate kuishi! Na dhahabu za Sheba

apewe yeye. Watu wamuombee yeye siku zote; Mungu ambariki daima. 16 Kuwepo
na nafaka nyingi katika ardhi; juu ya milima kuwe na mawimbi ya mimea. Matunda
yake yawe kama Lebanoni; watu wasitawi katika miji kama nyansi za kondeni. 17 Jina
lake lidumu milele; jina lake ilindelee kama vile jua ling'aavyo; watu wabarikiwe
katika yeye; mataifa yote wamwite mbarikiwa. 18 Yahwe Mungu, Mungu wa Israel,
atukuzwe, ambaye pekee hufanya mambo ya ajabu. 19 Jina lake tukufu litukuzawe
milele, nayo nchi yote ijazwe na utukufu wake. Amina, Amina. 20 Maombi ya Daudi
mwana wa Yese yamemalizika. Kutatu cha tatu

# 73

Zaburi ya Asafu. 1 Hakika Mungu ni mwema kwa Israeli, kwa wale walio na
moyo safi. 2 Lakini kwangu mimi, kidogo tu miguu yangu iteleze; miguu yangu
karibu iteleze kutoka kwangu 3 kwa sababu niliwaonea wivu wenye kiburi nilipoona
mafanikio ya waovu. 4 Kwa maana hawana maumivu hadi kufa kwao, lakini wana
nguvu na wameshiba. 5 Wako huru dhidi ya mizigo ya watu wengine; nao hawateswi
kama watu wengine. 6 Kiburi kinawapamba kama mkufu kwenye shingo zao; jeuri
huwavika kama vazi. 7 Katika upofu wa jinsi hii dhambi huja; mawazo maovu
hupita mioyoni mwao. 8 Wao hudhihaki na kuongea kwa namna ya uovu; kwa
kiburi chao hutishia mateso. 9 Wameweka vinywa vyao dhidi ya mbingu, na ndimi
zao hutanga tanga duniani. 10 Kwa hiyo watu wake huwageukia na maji yaliyojaa
hukaushwa. 11 Nao husema, “Mungu anajuaje? Yako maarifa kwake yeye aliye
juu?” 12 Fahamu: watu hawa ni waovu; mara zote hawajali, wakifanyika matajiri
na matajiri. 13 Hakika nimeutunza moyo wangu bure na nimenawa mikono yangu
pasipo kukosa. 14 Maana mchana kutwa nimeteswa na kuadhibiwa kila asubuhi.
15 Kama ningesema, “Ningesema mambo haya,” kumbe nigewasaliti kizazi hiki cha
watoto wenu. 16 Ingawa nilijaribu kuyaelewa mambo haya, yalikuwa ni magumu
sana kwangu. 17 Ndipo nilipoingia patakatifu pa Mungu na kuelewa hatma yao.
18 Hakika wewe huwaweka penye utelezi; huwaangusha mpaka palipoharibika.
19 Jinsi gani wamekuwa ukiwa kwa muda mfupi! Wamefika mwisho nao wamemaliza
kwa utisho. 20 Wao ni kama ndoto wakati wa mtu kuamka; Bwana, utakapo
inuka, utazidharau ndoto zao. 21 Maana moyo wangu ulipata uchungu, nami
nilijeruhiwa sana. 22 Nilikuwa mjinga na sijui neno; nilikuwa kama mnyama tu
mbele yako. 23 Lakini mimi nipo pamoja nawe daima; umenishika mkono wa kuume.
24 Utaniongoza kwa shauri lako na baadaye utanipokea katika utukufu. 25 Ni nani
niliye naye mbinguni isipokuwa wewe? Hakuna nimtamaniye duniani isipokuwa
wewe. 26 Mwili wangu na moyo wangu huwa dhaifu, bali Mungu ndiye nguvu ya
moyo wangu daima. 27 Wale walio mbali nawe wataangamia; utawaangamiza wote
wasio waaminifu kwako. 28 Lakini mimi, linipasalo kufanya ni kumkaribia Mungu.
Nimemfanya Bwana Yahwe kimbilio langu. Nami nitayatangaza matendo yako yote.

# 74

Zaburi ya Asafu. 1 Mungu, kwa nini umetukataa milele? Kwa nini hasira
yako inawaka dhidi ya kondoo wa malisho yako? 2 Wafikilie watu wako, ambao
uliwanunua siku nyingi zilizopita, kabila ambalo wewe umelikomboa liwe urithi
wako, na Milima Sayuni, mahali uishipo. 3 Uje utazame uharibifu kamili, uharibifu
ambao umefanywa na adui mahali patakatifu. 4 Washindani wako walivamia katikati
ya mahali pako maalumu; walipandisha bendera zao za vita. 5 Walipakatakata kwa
shoka kama katika msitu mnene. 6 Walipaharibu na kuvunja sanaa zilizonakshiwa
zote; walizivunja kwa shoka na nyundo. 7 Walipachoma patakatifu pako; walipanajisi
mahari unapoishi, wakigongagonga kwenye ardhi. 8 Walisema mioyoni mwao,

“Tutawaharibu wote.” Walichoma sehemu zako zote za kukutania katika nchi.
9 Sisi hatuoni tena ishara; hakuna tena nabii, na hakuna yeyote miongoni mwetu
ajuaye haya yatadumu kwa muda gani. 10 Mpaka lini, Mungu, adui atakurushia
wewe matusi? Je, atalitukana jina lako milele? 11 Kwa nini umerudisha nyuma
mkono wako, mkono wako wa kuume? Utoe mkono wako kwenye mavazi yako
na uwaangamize. 12 Lakini Mungu amekuwa mfalme wangu tangu enzi, akileta
wokovu tuniani. 13 Wewe uliigawa bahari; ulishambulia vichwa vya majitu ya kutisha
baharini majini. 14 Wewe ulishambulia vichwa vya lewiathani; na kumfanya awe
chakula cha viumbe hai jangwani. 15 Ulizifungulia chemchem na vijito; uliikausha
mito itiririkayo. 16 Mchana ni wako, na usiku ni wako pia; uliweka jua na mwezi
mahari pake. 17 Umeiweka mipaka ya nchi; umeumba majira ya joto na majira ya
baridi. 18 Kumbula vile adui alivyo vurumisha matusi kwako, Yahwe, na kwamba
watu wapumbavu wamelitukana jina lako. 19 Usimtoe njiwa afe kwa mnyama wa
porini. Usiusahau milele uhai wa watu wako walio onewa. 20 Kumbuka agano
lako, maana majimbo ya giza ya nchi yamejaa maeneo ya vurugu. 21 Usiwaache
walioonewa warudishwe kwa aibu; uwaache maskini na walioonewa walisifu jina
lako. 22 Inuka Mungu, itetee heshima yako; kumbuka wajinga wanavyokutukana
machana kutwa. 23 Usisahau sauti ya adui zako au kelele za wale wanaoendelea
kukuchafua.

# 75

Kwa kiongozi wa muziki; seti kwenye Al Tashheth. Zaburi ya Asafu, wimbo.
1 Tunatoa shukrani kwako, Mungu; tunatoa shukrani, maana wewe unaufunua
uwepo wako; watu huzungumza kuhusu kazi zako za ajabu. 2 Kwa wakati maalum
nitahukumu kwa haki. 3 Ingawa nchi na wenyeji wote watatikisika katika hofu,
ninaifanyia nchi nguzo za kutosha. Selah 4 Nilisema kwa wenye kiburi, “Msiwe
wenye kiburi,” na kwa waovu, “Msiinue mapembe. 5 Msiinue mapembe yenu kwenye
marefu; wala msizungumze kwa shingo ya kiburi.” 6 Sio kutoka mashariki au
magharibi, na wala sio kutoka jangwani ambako kuinuliwa kunakuja. 7 Bali Mungu
ni muhumkumu; humshusha huyu na kumuinua huyu. 8 Kwa kuwa Yahwe kashikilia
mkononi mwake kikombe cha mvinyo wenye povu, ambao umechanganywa na
vilolezo, naye huimimina. Hakika waovu wote wa duniani watakunywa mvinyo hadi
tone la mwisho. 9 Bali mimi nitaendelea kusema yale ambayo umeyatenda; nami
nitamwimbia sifa Mungu wa Yakobo. 10 Yeye husema, “Nitayakata mapembe yote ya
waovu, lakini mapembe ya wenye haki yatainuliwa.”

# 76

Kwa kiongozi wa muziki, kwenye vyombo vya nyuzi. zaburi ya Asafu, wimbo.
1 Mungu amefanya mwenyewe kujulikana katika Yuda; jina lake ni kuu katika Israeli.
2 Hema yake iko salemu; makao yake yako yako Sayuni. 3 Huko ndiko alivunja mishale
ya upinde, ngao, upanga, na silaha zingine za vita. Selah 4 Wewe unang'aa sana
na huufunua utukufu wako, ushukapo kutoka milimani, ambako uliwauwa mateka.
5 Wenye moyo shujaa walitekwa nyara; walilala mauti. Mashujaa wote walikuwa
wanyonge. 6 Kwa kukemea kwako, ewe Mungu wa Yakobo, wote gari na farasi
walilala mauti. 7 Wewe, ndiyo wewe, ni wa kuogopwa; ni nani awezaye kusimama
mbele yako wakati ukiwa na hasira? 8 Kutoka mbinguni wewe uliifanya hukumu yako
isikike; nchi iliogopa na ikaa kimya 9 wakati wewe, Mungu, ulipoinuka kutekeleza
hukumu na kuwaokoa wote wa nchi walio onewa. Selah 10 Hakika hukumu ya hasira
yako dhidi ya binadamu itakuletea wewe sifa; wewe hujifunga mwenyewe hasira
yako iliyo baki. 11 Wekeni nadhiri kwa Yahwe Mungu wenu na kuzihifadhi. Nao

wote wamzungukao yeye mleteeni zawadi yeye ambaye ni wa kuogopwa. 12 Yeye
huzikata roho za wakuu; huogopwa na wafalme wa nchi.

## 77

Kwa kiongozi wa muziki; baada ya manner ya Jeduthun. Zaburi ya Asafu.
1 Nitampazia Mungu sauti yangu, nitamuita Mungu kwa sauti yangu, na Mungu
wangu atanisikia. 2 Katika siku ya taabu nilimtafuta Bwana; usiku niliinua mikono
yangu, nayo haikuchoka. Moyo wangu ulikataa kufarijiwa. 3 Ningali nikiugua
nilielekeza mawazo yangu kwa Mungu. Nilimfikiria Mungu nilipokuwa dhaifu.
Selah 4 Uliyafanya macho yangu yasisinzie; nilisumbuka sana kuongea. 5 Nilifikiri
kuhusu siku za kale, kuhusu mambo yaliyopita muda mrefu. 6 Wakati wa usiku
niliukumbuka wimbo niliouimba mara moja. Nilifikiria kwa makini na kujaribu
kuelewa kile kilichokuwa kimetokea. 7 Je, Mungu atanikataa milele? Je, hatanionesha
tena huruma? 8 Je, uaminifu wa agano lake ulikuwa umetoweka milele? Je, ahadi
yake imeshindwa milele? 9 Je, Mungu amesahau kuwa mwenye neema? Je, hasira
yake imeifunga huruma yake? Selah 10 Nilisema, "Hii ni huzuni yangu: mabadiliko
ya mkono wa kuume wa Aliye Juu dhidi yetu." 11 Lakini nitayakumbuka matendo
yako, Yahwe; nitafikiri kuhusu matendo yako makuu yaliyopita. 12 Nitayatafakari
matendo yako yote nami nitayaishi. 13 Njia yako, Mungu, ni takatifu; ni mungu
gani wa kulinganishwa na Mungu wetu aliye mkuu? 14 Wewe ni Mungu utendaye
maajabu; wewe umeonesha nguvu zako kati ya mataifa. 15 Uliwapa watu wako
ushindi kwa uweza wako mkuu - ukoo wa Yakobo na Yusufu. Selah 16 Maji yalikuona
wewe, Mungu; maji yalikuona wewe, nayo yakaogopa; vina vya maji vilitetemeka.
17 Mawingu yalitiririsha maji chini; anga zito lilitoa sauti; mishale yako ilipita kati.
18 Sauti yako kama ya radi ilisikika katika upepo; radi iliwasha dunia; nchi iliogopa
na kutetemeka. 19 Njia yako ilipita baharini na mapito yako katika maji mengi, lakini
alama za miguu yako hazikuonekana. 20 Uliwaongoza watu wako kama kundi kwa
mkono wa Musa na Haruni.

## 78

Zaburi ya Asafu. 1 Watu wangu, sikieni mafundisho yangu, sikilizeni maneno
ya kinywa changu. 2 Nitafungua kinywa changu katika mifano; nitaimba kuhusu
mambo yaliyofichika yahusuyo yaliyopita. 3 Haya ni mambo ambayo tumeyasikia na
kujifunza mambo ambayo mababu zetu wametuambia sisi. Hatutawaficha uzao wao.
4 Tutawaambia kizazi kijacho kuhusu sifa anazostahili Yahwe kwa matendo yake,
nguvu zake, na maajabu ambayo ameyafanya. 5 Kwa kuwa yeye alianzisha agano la
amri katika Yakobo na sheria maalumu katika Israeli. Yeye aliamuru mababu zetu
kuwa walipaswa kuzifundisha kwa watoto wao. 6 Aliamuru hivi ili kwamba kizazi
kijacho kiweze kuzijua amri zake, ili wawafundishe wana ambao bado hawajazaliwa.
7 Kisha wangeweka tumaini lao katika Mungu na kutokusahau matendo yake bali
wazishike amri zake. 8 Ndipo wasingekuwa kama mababu zao, ambao walikuwa
wakaidi na wenye uasi, kizazi ambacho mioyo yao haikuwa kamilifu, na ambao
roho zao hazikuwa na nia thabiti na aminifu kwa Mungu. 9 Waefraimu walikuwa
na silaha na upinde, lakini walikimbia siku ya vita. 10 Hawakutunza agano na
Mungu, na walikataa kutii sheria yake. 11 Walisahau matendo yake, mambo ya
ajabu ambayo yeye amewaonesha wao. 12 Walisahau mambo ya ajabu aliyofayafanya
machoni pa mababu zao katika nchi ya Misri, katika ardhi ya Soani. 13 Aliigawa
bahari na akawaongoza katikati ya bahari; aliyafanya maji yasimame kama kuta.
14 Wakati wa mchana aliwaongoza kwa wingu na usiku wote kwa nuru ya moto.
15 Alipasua miamba jangwani, na aliwapa maji mengi, ya kutosha kujaza vina

virefu vya bahari. 16 Alifanya maporomoko ya maji kutiririka tokea mwambani na
aliyafanya maji yatiririke kama mito. 17 Lakini bado waliendelea kutenda dhambi
dhidi yake, wakiasi dhidi ya Aliye Juu katika jangwa. 18 Walimjaribu Mungu
mioyoni mwao kwa kuomba chakula cha kuwatosheleza hamu zao. 19 Waliongea
dhidi ya Mungu; walisema, "Kweli Mungu anaweza kuweka meza ya chakula kwa
ajili yetu jangwani? 20 Tazama, wakati alipoupiga mwamba, maji yalibubujika,
mito ikafurika. Lakini anaweza kutoa mkate tena? Ataweza kuleta nyama kwa
watu wake?" 21 Yahwe aliposikia haya, alikasirika; moto wake uliwaka dhidi ya
Yakobo, hasira yake ikamshambulia Israeli, 22 kwa sababu hawakumwamini Mungu
na hawakuamini katika wokovu wake. 23 Lakini yeye bado aliziamuru mbingu
juu na kufungua milango ya mbingu. 24 Aliwanyeshea mana ili wale, na aliwapa
nafaka kutoka mbinguni. 25 Watu walikula mikate ya malaika. Aliwatumia chakula
kingi. 26 Alisababisha upepo wa mashariki kupiga mawinguni, na kwa uweza wake
aliuongoza upepo wa kusini. 27 Aliwanyeshea nyama kama mavumbi, na ndege
kama wingi wa mchanga wa baharini. 28 Walianguka katikati ya kambi yao, na
maeneo yote karibu na hema zao. 29 Hivyo walikula na walishiba. Maana aliwapa
kile walichokitamani sana. 30 Lakini walikuwa bado hawajatosheka; chakula chao
kilikuwa bado kinywani mwao. 31 Ndipo hasira ya Mungu iliwashambulia na kuwaua
wenye nguvu kati yao. Aliwaangusha chini vijana wa Israeli. 32 Licha ya hili,
waliendelea kutenda dhambi na hawakuyaamini matendo yake ya ajabu. 33 Hivyo
Mungu alizikatisha siku zao; miaka yao ilijawa na hofu. 34 Wakati wowote Mungu
alipowataabisha, nao waligeuka na kumtafuta yeye kwa bidii. 35 Walikumbuka kuwa
Mungu alikuwa mwamba wao na kuwa Mungu Aliye Juu Sana alikuwa mwokozi
wao. 36 Lakini walimsifia tu kwa vinywa vyao na kumdanganya kwa maneno yao.
37 Maana mioyo yao haikuwa thabiti kwake, na hawakuwa waaminifu kwa agano
lake. 38 Lakini yeye, kwa kuwa alikuwa alikuwa na huruma, aliwasamehe uovu wao
na hakuwaangamiza. Ndiyo, wakati mwingi aliizuia hasira yake na hakuionesha
ghadhabu yake yote. 39 Alikumbuka kuwa waliumbwa kwa mwili, upepo ambao
hupita nao haurudi. 40 Mara ngapi wameasi dhidi yake jangwani na kumuhuzunisha
nyikani! 41 Tena na tena walimjaribu Mungu na wakamtilia mashaka Mtakatifu wa
Israeli. 42 Hawakufikiria kuhusu uweza wake, jinsi alivyo waokoa dhidi ya adui
43 alipofanya ishara za kutisha katika Misri na maajabu yake katika konde la Soani.
44 Aligeuza mito ya Wamisri kuwa damu ili wasipate kunywa kutoka katika vijito
vyao. 45 Alituma makundi ya inzi yaliyowavamia na vyura ambao walisambaa katika
nchi yao. 46 Aliwapa mazao yao panzi na kazi yao nzige. 47 Aliiharibu mizabibu yao
kwa mvua ya mawe na miti ya mikuyu kwa mvua ya mawe zaidi. 48 Aliinyeshea
mifugo yao mvua ya mawe na alirusha radi ya umeme ikapiga mifugo yao. Ukali
wa hasira yake ulielekea dhidi yao. 49 Alituma gadhabu, uchungu na taabu kama
wakala aletaye maafa. 50 Aliifanyia njia hasira yake; hakuwakinga dhidi ya kifo
bali aliwakabidhi kwa pigo. 51 Aliwaua wazaliwa wote wa kwanza katika Misri,
wazaliwa wa kwanza wa nguvu zao katika mahema ya Hamu. 52 Aliwaongoza
nje watu wake mwenyewe kama kondoo na aliwaelekeza kupitia jangwani kama
kundi. 53 Aliwaongoza salama na pasipo na woga, lakini bahari iliwaelemea adui
zao. 54 Kisha aliwaleta mpaka wa nchi yake takatifu, kwenye mlima huu ambao
aliutwaa kwa mkono wake wa kuume. 55 Aliwafukuza mataifa mbele yao na akawapa
urithi wao. Aliwakalisha makabila ya Israeli katika mahema yao. 56 Lakini bado
walimjaribu na walimkaidi Mungu Aliye Juu na hawakushika amri zake takatifu.
57 Hawakuwa waaminifu na walienenda katika hila kama baba zao; walikuwa sio wa
kutegemewa kama upinde mbovu. 58 Kwa maana walimkasirisha kwa mahali pao pa

juu na walimgadhabisha hata akawa na hasira ya wivu kwa miungu yao. 59 Mungu
aliposikia hili, alikasirika na alimkataa kabisa Israeli. 60 Alipaacha patakatifu pa Shilo,
na hema alikoishi kati ya watu. 61 Aliruhusu nguvu zake kutekwa na kuutoa utukufu
wake mkononi mwa adui. 62 Aliukabidhi upanga watu wake, na aliukasirikia urithi
wake. 63 Moto uliwavamia vijana wao wa kiume, na vijana wao wa kike hawakuwa
na nyimbo za harusi. 64 Makuhani wao waliangushwa kwa upanga, na wajane
wao hawakulia. 65 Kisha Bwana aliamshwa kama aliyetoka usingizini, kama shujaa
apigaye kelele kwa sababu ya mvinyo. 66 Aliwarudisha adui zake nyuma; aliwaweka
kwenye aibu ya milele. 67 Aliikataa hema ya Yusufu, na hakulichagua kabila la
Efraimu. 68 Alilichagua kabila la Yuda na Mlima Sayuni aliyoupenda. 69 Alipajenga
patakatifu pake kama mbinguni, na kama nchi aliyoiimarisha milele. 70 Alimchagua
Daudi, mtumishi wake, alimchukua kutoka zizi la kondoo. 71 Alimtoa kutoka katika
kufuata kondoo pamoja na wana wao, na kumweka kuwa mchungaji wa Yakobo,
watu wake, na Israeli, urithi wake. 72 Daudi aliwachunga kwa uadilifu wa moyo
wake, naye aliwaongoza kwa ujuzi wa mikono yake.

# 79

1 Zaburi ya Asafu. Mungu, Mataifa ya kigeni yameingia kwenye urithi wako;
wamelinajisi hekalu lako takatifu; wameigeuza Yerusalemu kuwa chungu cha
magofu. 2 Wamezitoa maiti za watumishi wako ziwe chakula cha ndege wa angani,
miili ya watakatifu wako iwe chakula cha wanyama wa nchi. 3 Wamemwaga
damu zao kama maji sehemu zote za Yesrusalemu, na hakuwepo wa kuwazika.
4 Sisi tumekuwa aibu kwa majirani zetu, tukidhihakiwa na kuzomewa na wale
wanaotuzunguka. 5 Mpaka lini Yahwe? Utabaki kuwa na hasira milele? Ni kwa
muda gani hasira yako ya wivu itawaka kama moto? 6 Mwaga hasira yako juu ya
mataifa ambayo hayakujui wewe na ufalme ambao hauliiti jina lako. 7 Kwa maana
walimvamia Yakobo na waliharibu kijiji chake. 8 Usiendelee kukumbuka dhambi
za baba zetu dhidi yetu; matendo yako ya huruma yaje kwetu, maana tuko chini.
9 Utusaidie, Mungu wa wokovu wetu, kwa ajili ya utukufu wa jina lako; utuokoe na
usamehe dhambi zetu kwa ajili ya jina lako. 10 Kwa nini mataifa yalazimike kusema,
“Mungu wao yuko wapi?” Damu ya watumishi wako ambayo ilimwagwa na ilipize
kisasi juu ya mataifa mbele ya macho yako. 11 Kilio cha wafungwa na kije mbele
zako; kwa uweza wa nguvu zako uwaweke ai wana wa mauti. 12 Uwalipize majirani
zetu vifuani mwao mara saba zaidi ya walivyo kutukana wewe, Bwana. 13 Hivyo
sisi watu wako na kondoo wa malisho yako tutakushukuru milele. Tutazisimulia sifa
zako kwa vizazi vyote.

# 80

Kwa kiongozi wa muziki, seti kwenye mtindo wa Shoshannim Eduth. Zaburi ya
Asafu. 1 Usikie, Mchungaji wa Israel, wewe uliye muongoza Yusufu kama kundi;
wewe uketiye juu ya makerubi, utuangazie! 2 Machoni pa Efraimu na Benjamini na
Manase, uziinue nguvu zako; njoo na utuokoe. 3 Mungu, uturejeshe sisi; uangaze
uso wako juu yetu, nasi tutaokolewa. 4 Yahwe Mungu wa majeshi, mpaka lini
utawakasirikia watu wako wanapoomba? 5 Umewalisha wa mkate wa machozi na
umewapa machozi ili wanywe katika kiasi kikubwa. 6 Umetufanya kitu kwa ajili ya
majirani zetu kubishania, na maadui zetu hucheka kuhusu sisi kati yao. 7 Mungu
wa majeshi, uturejeshe sisi; nasi tutaokolewa. 8 Wewe ulileta mzabibu kutoka Misri;
ukawafukuza mataifa na ukaupanda. 9 Uliisafisha ardhi kwa ajil yake; nao ulipata
mzizi na kuijaza nchi. 10 Milima ilifunikwa kwa kivuli chake, mierezi ya Mungu
kwa matawi yake. 11 Ilieneza matawi yake mbali kama bahari na mashina yake

mpaka kwenye Mto Euphrates. 12 Kwa nini umezibomoa kuta zake hata wapitao
karibu huyachuma matunda yake. 13 Ngurue wa msituni wanauharibu, na wanyama
wa kondeni wanaula. 14 Urudi, Ee Mungu wa majeshi; kutoka mbinguni utazame
chini na uuangalie na kuujali huu mzabibu. 15 Huu ni mzizi ambao mkono wako
wa kuume umeupanda, mashina ambayo wewe uliyafanya yakue. 16 Yamekatwa na
kuchomwa; yameangamia kwa sababu ya kukemea kwako. 17 Mkono wako na uwe
juu ya mtu aliye mkono wako wa kuume, kwa mwana wa mtu uliyemfanya imara
kwa ajili yako mwenyewe. 18 Ndipo hatuta kuacha wewe; utuhuishe, nasi tutaliita
jina lako. 19 Yahwe, Mungu wa majeshi, uturejeshe sisi; utuangazie nuru ya uso
wako, nasi tutaokolewa.

# 81

Kwa kiongozi wa muziki; seti kwenye mtindo wa Gittith. 1 Mwimbieni Mungu aliye
nguvu yetu kwa sauti; pigeni kelele za furaha kwa Mungu wa Yakobo. 2 Imbeni
wimbo na pigeni matari, kinubi chenye sauti nzuri pamoja na kinanda. 3 Pigeni
panda mwandamo wa mwezi, katika siku ya mbalamwezi, mwanzoni mwa sikukuu.
4 Kwa kuwa ni agizo kwa Israeli, amri iliyotolewa na Mungu wa Yakobo. 5 Aliitoa
kama maelekezo kwa Yusufu alipoenda katika nchi ya Misri, ambako nilisikia sauti
ambayo sikuweza kuitambua: 6 "Niliutua mzigo kutoka mabegani mwake; mikono
yake ilipumzishwa kubeba kikapu. 7 Katika dhiki yako uliniita, nami nikakusaidia;
nilikujibu kutoka katika wingu jeusi la radi. Nilikujaribu kwenye maji ya Meriba.
Selah 8 Sikilizeni, watu wangu, nami nitawaonya, Israeli, kama tu ugalinisikiliza!
9 Lazima kati yenu kusiwepo na mungu wa kigeni; haupaswi kumwabudu mungu
wa kigeni. 10 Mimi ni Yahwe niliyekutoa katika nchi ya Misri, fungua sana kinywa
chako, nami nitakijaza. 11 Lakini watu wangu hawakusikiliza maneno yangu; Israeli
hawakunitii. 12 Nikawaacha waende katika katika njia yao wenyewe ya ukaidi ili
kwamba waweze kufanya kinachoonekana sahihi kwao. 13 Oh, laiti watu wangu
wangenisikiliza mimi; oh, watu wangu wangelitembea katika njia yangu. 14 Kisha
ningewatiisha adui zao haraka na kugeuzia mkono wangu dhidi ya watesi wao.
15 Wale wanaomchukia Yahwe katika hofu na waanguke chini mbele zake! Wawe
wanyonge milele. 16 Ningewalisha Israeli kwa ngano bora; Ningewatosheleza kwa
asali itokayo mwambani."

# 82

Zaburi ya Asafu. 1 Mungu amesimama katika kusanyiko la mbinguni; katikati ya
miungu anahukumu. 2 Hata lini mtahukumu bila haki na kuonesha upendeleo kwa
waovu? Selah 3 Wateteeni maskini na yatima; dumisheni haki kwa aliyetaabishwa na
fukara. 4 Muokoeni maskini na muhitaji; watoeni mkononi mwa waovu. 5 Hawajui
wala hawaelewi; hutembea gizani; misingi yote ya nchi imebomoka. 6 Mimi nilisema,
"Ninyi ni miungu, na ninyi nyote wana wa Mungu aliye Juu. 7 Hata hivyo mtakufa
kama wanadamu na mtaanguka kama mmoja wa wakuu." 8 Uinuke, Ee Mungu,
uihukumu nchi, maana unaurithi katika mataifa yote.

# 83

Wimbo. Zaburi ya Asafu. 1 Ee Mungu, usikae kimya! usitupuuze na kustarehe, Ee
Mungu. 2 Tazama, adui zako wanafanya vurugu, na wale wakuchukiao wameinua
vichwa vyao. 3 Wanafanya hila juu ya watu wako na kwa pamoja kupanga njama
dhidi ya wale uwalindao. Wamesema, 4 "Njoni na tuwaangamize wao kama taifa.
Kisha jina la Israeli halitakumbukwa." 5 Wamepanga njama pamoja wakiwa na
mkakati mmoja; wamefanya muungano dhidi yako. 6 Hii inajumuisha hema za

Edomu na Waishmaeli, na watu wa Moabu na Wahagari, ambao wamepanga njama
pamoja nao 7 Gebal, Amoni, Amaleki; pia inajumuisha Filisti na wenyeji wa Tiro.
8 Ashuri pia ameshirikina nao; wanawasaidia wana wa Lutu. Serah 9 Ufanye kwao
kama ulivyofanya kwa Midiani, kama ulivyofanya kwa Sisera na kwa Yabini kwenye
Mto Kishoni. 10 Waliangamizwa kule Endori na wakawa kama mbolea juu ya chi.
11 Uvifanye vyeo vyao kama Oreb na Zeeb, na wakuu wao wote kama Zeba na
Zalmuna. 12 Wao walisema, natujimilikishe malisho ya Mungu." 13 Ee Mungu wangu,
uwafanye kama mavumbi ya kisulisuli, kama makapi mbele ya upepo, 14 Kama moto
uteketezao msitu, na kama miali ya moto iwakayo milimani. 15 Uwafuatie kwa tufani
yako, na kuwafadhaisha kwa dhoruba yako. 16 Uwajaze nyuso zao kwa aibu ili
kwamba waweze kulitafuta jina lako, Yahwe. 17 Nao waaibishwe na kufadhaishwa
milele; waangamizwe katika aibu. 18 Kisha watajua kwamba ni wewe pekee, Yahwe,
Uliye Juu ya nchi yote.

# 84

Kwa kiongozi wa muziki; seti kwenye mtindo wa Gittith. Zaburi ya wana wa
Kora. 1 Ni jinsi gani maskani yako yapendeza, Ewe Yahwe wa Majeshi! 2 Ninashauku
ya kuingia nyumbani mwa Yahwe, nimechoka sana kwa sababu ninatamani sana
kuwa nyumani mwako. Moyo wangu na mwili wangu wote wakuita wewe Mungu
uliye hai. 3 Hata Shomoro naye amepata nyumba yake na mbayuwayu amejipatia
kiota kwa ajili yake mwenyewe mahali awezapo aweza kuweka makinda yake
karibu na madhabahu yako, Ee Yahwe wa majeshi, Mfalme wangu, na Mungu
wangu. 4 Wamebarikiwa wale ambao huishi katika nyumba yako; nao hukusifu
wewe siku zote. Selah 5 Amebarikiwa mtu yule ambaye nguvu zake ziko katika
wewe, katika moyo wake mna njia kuu ziendazo mpaka Sayuni. 6 Wanapopita katika
bonde la machozi, hupata chemchem ya maji kwa ajili ya kunywa. Mvua ya vuli
hulivika baraka. 7 Huendelea toka nguvu hadi nguvu; kila mmoja wao katika sayuni
huonekana mbele ya Mungu. 8 Yahwe Mungu wa majeshi, sikia maombi yangu;
Mungu wa Yakobo, usikilize nisemacho! Selah 9 Ee Mungu, uiangalie ngao yetu;
uwaangalie wapakwa mafuta wako. 10 Kwa maana siku moja katika nyumba yako
ni bora kuliko siku elfu mahali pengine. Ni bora niwe mlinzi wa mlango katika
nyumba ya Mungu wangu, kuliko kuishi katika mahema ya waovu. 11 Kwa kuwa
Yahwe Mungu ni jua letu na ngao yetu; Yahwe atatoa neema na utukufu; hazuii zuri
lolote kwa wale ambao hutembea katika uadilifu. 12 Yahwe wa majeshi, amebarikiwa
mtu yule anaye kutumainia wewe.

# 85

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya wana wa Kora. 1 Yahwe, wewe umeonesha
fadhilia kwenye nchi yako; umeurejesha ustawi wa Yakobo. 2 Umesamehe dhambi
ya watu wako; umezisitiri dhambi zao zote. Selah 3 Umeondoa ghadhabu yako
yote; umeiacha hasira yako kali. 4 Uturejeshe sisi, Ee Mungu wa wokovu wetu, na
uikomeshe chuki yako juu yetu. 5 Je! Utaendelea kuwa na hasira juu yetu milele?
utadumisha hasira kizazi chote kijacho? 6 Je, hautatuhuisha tena? Kisha watu wako
watafurahia katika wewe. 7 Utuoneshe sisi uaminifu wa agano lako, Yahwe, utupe
sisi wokovu wako. 8 Nitasikiliza yale Yahwe Mungu asemayo, maana yeye atafanya
amani pamoja na watu wake, wafuasi wake waminifu. Lakini lazima wasirudi tena
katika njia za kipumbavu. 9 Hakika wokovu wake u karibu na wale wanao mwabudu
yeye; kisha utukufu utabaki katika nchi yetu. 10 Uaminifu wa agano na uaminifu
vimekutana pamoja; haki na amani vimebusiana. 11 Uaminifu unatoa chemchem
kutoka ardhini, na haki hutazama chini kutoka mawinguni. 12 Ndiyo, Yahwe atatoa

baraka zake njema, na nchi itatoa mazao yake. [13] Haki itaenda mbele zake na kufanya njia kwa ajili ya nyayo zake.

# 86

Maombi ya Daudi. [1] Sikia, Ee Yahwe, na unijibu, kwa kuwa ni maskini na mnyonge.
[2] Unilinde, maana mimi ni mwaminifu; Mungu wangu, umuokoe mtumishi wako
anayekuamini. [3] Unihurumie, Bwana, maana ninakulilia wewe mchana kutwa.
[4] Umfurahishe mtumishi wako, maana ni kwako, Bwana, ninaomba. [5] Wewe, Bwana,
ni mwema, na uko tayari kusamehe, na huonesha huruma kubwa kwa wale wanao
kulilia wewe. [6] Yahwe, sikiliza maombi yangu; sikia sauti ya ombi langu. [7] Katika
siku ya shida ninakuita wewe, kwa maana utanijibu. [8] Katikati ya miungu hakuna
wa kufananishwa na wewe, Bwana. Hakuna matendo kama matendo yako. [9] Mataifa
yote ambayo umeyafanya yatakuja kwako na kusujudu mbele zako, Bwana. nao
wataliheshimu jina lako. [10] Kwa kuwa wewe ni mkuu na utendaye mambo ya ajabu;
wewe pekee ndiwe Mungu. [11] Unifundishe njia zako, Yahwe. Kisha nitatembea
katika kweli yako. Unifanye kukuheshimu wewe. [12] Bwana Mungu wangu, nitakusifu
kwa moyo wangu wote; nitalitukuza jina lako milele. [13] Kwa maana uaminifu wa
agano lako ni mkuu kwangu; wewe umeokoa uhai wangu kutoka chini kuzimuni.
[14] Ee Mungu, wenye kiburi wameinuka dhidi yangu. Kundi la watu wenye vurugu
wanautafuta uhai wangu. Nao hawakuheshimu wewe. [15] Lakini wewe, Bwana,
ni mwenye huruma na neema, hukasiliki haraka, na mwingi katika uaminifu wa
agano lako na kweli. [16] Unigeukie na unihurumie; mpe nguvu zako mtumishi wako;
umuokoe mwana wa mjakazi wako. [17] Unioneshe ishara ya fadhila zako. Kisha wale
wanichukiao wataziona na kuaibishwa kwa sababu yako; Yahwe, umenisaidia na
kunifariji.

# 87

Zaburi ya wana wa Kora; wimbo. [1] Mji aliouanzisha umesimama juu ya mlima
mtakatifu; [2] Yahwe anapenda zaidi malango ya Sayuni kuliko mahema yote ya
Yakobo. [3] Mambo matukufu yamesemwa kwako, mji wa Mungu. Selah [4] Ninataja
Rahabu na Babeli kwa wafuasi wangu. Tazama, Filisti, na Tiro, pamoja na Ethiopia
nao watasema, 'Huyu alizaliwa humo.'" [5] Itasemwa juu ya Sayuni, "Kila mmoja wa
hawa alizaliwa katika yeye; na yeye Aliye Juu atamuimarisha. [6] Yahwe anaandika
katika kitabau cha sensa ya mataifa, "Huyu alizaliwa humo." Selah [7] Hivyo waimbaji
na wachezaji kwa pamoja waseme, "chemchem zangu zimo kwako."

# 88

Wimbo, Zaburi ya wana wa Kora; kwa kiongozi wa muziki; seti kwenye mtindo
wa Mahalath Leannoth. Zaburi ya Heman mu Ezrahite. [1] Yahwe, Mungu wa wokovu
wangu, ninalia mchana na usiku mbele zako. [2] Sikiliza maombi yangu; utazame
kulia kwangu. [3] Maana nimejawa taabu, na uhai wangu umefika kuzimuni. [4] Watu
hunichukulia kama wale waendao chini shimoni; mimi ni mtu asiye na nguvu.
[5] Nimetelekezwa miongoni mwa wafu; niko kama mfu alalaye katika kaburi, wao
ambao wewe huwajari tena kwa sababu wametengwa mbali na nguvu zako. [6] Wewe
umeniweka katika sehemu ya chini kabisa ya shimo, sehemu yenye giza na kilindini.
[7] Gadhabu yako yanielemea, na mawimbi yako yote yanatua juu yangu. Selah [8] Kwa
sababu yako, wale wanijuao wote hunikwepa. Umenifanya wakutisha machoni pao.
Nimefungwa na siwezi kutoroka. [9] Macho yangu yamefifia kutokana na shida; kila
siku nakuita wewe, Yahwe; ninakunyoshea wewe mikono yangu. [10] Je! utafanya
miujiza kwa ajili ya wafu? Wale waliokufa watafufuka na kukusifu wewe? Selah

11 Uaminifu wa agano lako utatangazwa kaburini? au uaminifu wako mahali pa
wafu? 12 Matendo yako ya ajabu yatajulikana gizani? au haki yako katika mahali pa
usahaulifu? 13 Lakini ninakulilia wewe, Yahwe; wakati wa asubuhi maombi yangu
huja kwako. 14 Yahwe, kwa nini unanikataa? Kwa nini unauficha uso wako mbali
nami? 15 Nimekuwa nikiteswa kila siku na hatihati ya kifo tangu ujana wangu.
Nimeteseka dhidi ya hofu yako kuu; ninakata tamaa. 16 Matendo yako ya hasira
yamepita juu yangu, na matendo yako ya kutisha yameniangamiza. 17 Siku zote
yananizingira mimi kama maji; yote yamenizunguka mimi. 18 Wewe umemuondoa
kwangu kila rafiki na anijuaye. Na sasa anijuaye pekee ni giza.

# 89

Zaburi ya Ethan Muezrahite. 1 Nitimba sifa za matendo ya uaminifu wa
agano milele. Nitatangaza kweli yako kwa vizazi vijavyo. 2 Maana nimesema,
“Uaminifu wa agano umeimarishwa milele; na kweli yako umeiimarisha mbinguni.”
3 “Nimefanya agano na wateule wangu, nimeapa kiapo kwa Daudi mtumishi wangu.
4 Nitauimarisha uzao wako milele, na nitauimarisha utawala wako vizazi vyote.”
Selah 5 Mbingu husifu maajabu yako, Yahwe; kweli yako inasifiwa katika kusanyiko
la watakatifu. 6 Maana ni nani katika mbingu aweza kulinganishwa na Yahwe?
Ambaye kati ya wana wa miungu ni kama Yahwe? 7 Ni Mungu anaye heshimiwa
sana katika baraza la watakatifu naye ni wakutisha kati ya wote wanao mzunguka.
8 Yahwe, Mungu wa majeshi, ni nani aliye na nguvu kama wewe, Yahwe? Kweli yako
inakuzunguka. 9 Wewe huitawala bahari yenye nguvu; mawimbi yainukapo, wewe
huyatuliza. 10 Ulimwangamiza Rahabu kama mmoja aliye uliwa. Uliwatawanya adui
zako kwa mkono wako wenye nguvu. 11 Mbingu ni zako wewe, na nchi pia. Uliiumba
dunia na vyote vilivyomo. 12 Uliumba kaskazini na kusini. Tabori na Hermoni
hulifurahia jina lako. 13 una mkono wa uweza na mkono wenye nguvu, na mkono
wako wa kuume uko juu. 14 Haki na hukumu ni msingi wa kiti chako. Uaminifu wa
agano lako na uaminifu huja mbele zako. 15 Wamebarikiwa watu wakuabuduo wewe!
Yahwe, wanatembea katika nuru ya uso wako. 16 Siku zote wanafurahia katika jina
lako, na katika haki yako wanakutukuza wewe. 17 Wewe ni fahari ya nguvu zao,
na kwa nguvu zako tu washindi. 18 Maana ngao zetu ni za kwako Yahwe; mfalme
wetu ni wa Mtakatifu wa Israeli. 19 Muda mrefu uliopita ulizungumza na waaminfu
wako katika maono; ulisema, “Nimeweka taji juu ya mwenye nguvu; nimemuinua
aliyechaguliwa kutoka kati ya watu. 20 Nimemchagua Daudi mtumishi wangu; kwa
mafuta yangu matakatifu nimempaka yeye. 21 Mkono wangu utamsaidia yeye; mkono
wangu utamtia nguvu. 22 Hakuna adui atakaye mdanganya; hakuna mwana wa
uovu atakaye muonea. 23 Nitawaangamiza adui zake mbele yake; nitawaua wale
wamchukiao. 24 Kweli yangu na uaminifu wa agano vitakuwa pamoja naye; kupitia
jina langu atakuwa mshindi. 25 Nitaweka mkono wake juu ya bahari na mkono wake
wa kuume juu ya mito. 26 Yeye ataniita, 'Wewe ni Baba yangu, Mungu wangu, na
mwamba wa wokovu wangu.' 27 Nitamjalia kuwa kama mzaliwa wangu wa kwanza,
aliye inuliwa zaidi juu ya wafalme wa nchi. 28 Nitaongeza uaminifu wa agano
langu kwake milele; na agano langu pamoja naye litakuwa salama. 29 Nitaufanya
uzao wake kudumu milele na kiti chake cha enzi kitadumu kama mbingu zilizo
juu. 30 Ikiwa watoto wake wataziacha sheria zangu na kutokutii amri zangu, 31 na
kama watazivunja sheria zangu na kutokuzishika amri zangu, 32 ndipo nitauadhiu
uasi wao kwa fimbo na uovu wao kwa makofi. 33 Lakini sitauondoa kwake upendo
wangu thabiti wala kutokuwa mwaminifu kwa ahadi yangu. 34 Sitavunja agano
langu wala kubadilisha maneno ya midomoni mwangu. 35 Mara moja na kwa

yote, nimeapa kwa utakatifu wangu sitamdanganya Daudi: 36 uzao wake utaendelea
milele na kiti chake cha enzi kama vile jua mbele yangu. 37 Kitaimarishwa milele
kama mwezi, shahidi mwaminifu mawinguni." Selah 38 Lakini wewe umemtupa
na kumkataa; umemkasirikia mfalme mpakwa mafuta wako. 39 Wewe umelikataa
agano la mtumishi wako. Umeinajisi taji yake ardhini. 40 Umevunja kuta zake
zote. Umeharibu ngome yake. 41 Wapita njia wote wamemuibia, amekuwa kitu
chenye kinyaa kwa majirani zake. 42 Umeinua mkono wa kuume wa adui zake;
umewafurahisha adui zake wote. 43 Umeyageuza makali ya upanga wake. Na
hukumfanya asimame awapo vitani. 44 Umeimaliza fahari yake; umekitupa ardhini
kiti chake cha enzi. 45 Umefupisha siku za ujana wake. Umemfunika kwa aibu. Selah
46 Mpaka lini, Yahwe? utajificha, milele? Mpaka lini hasira yako itawaka kama moto?
47 Oh, fikiria jinsi muda wangu ulivyo mfupi, na ni kwa ajili gani umewaumba wana
wote wa wanadamu wasio na manufaa! 48 Ni nani aweza kuishi na asife, au atakaye
iokoa nafsi yake dhidi ya mkono wa kuzimu? Selah 49 Bwana, yako wapi matendo
yako ya zamani ya uaminifu wa agano ambayo ulimwapia Daudi katika kweli yako?
50 Kumbuka, Bwana, watumishi wako walivyodhihakiwa na vile nilivyo vumilia
moyoni mwangu matusi mengi dhidi ya mataifa. 51 Maadui zako wanavurumiza
matusi, Yahwe; wanadhihaki nyayo za mpakwa mafuta wako. 52 Atukuzwe Yahwe
milele. Amina na Amina. Kitabu cha Nne

# 90

Maombi ya Musa mtu wa Mungu. 1 Bwana, wewe umekuwa kimbilio letu vizazi
vyote. 2 Kabla milima haijaumbwa, wala haujaumba nchi na dunia, tangu milele
na milele, wewe ni Mungu. 3 Humrudisha mtu mavumbini, na kusema, "Rudi, ewe
uzao wa mwanadmu. 4 Kwa maana miaka elfu machoni pako ni kama jana ipitapo,
na kama saa wakati wa usiku. 5 Huwafagia kama vile kwa mafuliko nao hulala; na
wakati wa asubuhi wako kama majani yameayo. 6 Asubuhi yachipuka na kumea;
jioni yakatika na kukauka. 7 Hakika, tumeangamizwa kwa hasira yako, na gadhabu
yako inatuogopesha sana. 8 Umeudhihirisha uovu wetu mbele zako, na dhambi zetu
zilizofichika katika nuru ya uwepo wako. 9 Uhai wetu unatoweka chini ya gadhabu
yako; Miaka yetu inapita haraka kama pumzi. 10 Miaka yetu ni sabini, au themanini
tukiwa na afya; lakini hata hivyo miaka yetu mizuri imetiwa alama ya taabu na
huzuni. Ndiyo, inapita haraka, kisha tunatoweka. 11 Ni nani ajuaye kiwango cha
hasira yako, na ghadhabu yako ambayo iko sawa na hofu yako? 12 Hivyo utufundishe
sisi kuyafikiria maisha yetu ili kwamba tuweze kuishi kwa hekima. 13 Ugeuke, Ee
Yahwe! Mpaka lini itakuwa hivi? Uwahurumie watumishi wako. 14 Ututosheleze
sisi wakati wa asubuhi kwa uaminifu wa agano lako ili kwamba tuweze kufurahi na
kushangilia siku zote za maisha yetu. 15 Utufurahishe kwa uwiano sawa na zile siku
ulizo tutesa na kwa ile miaka tuliyopitia taabu. 16 Watumishi wako na waione kazi
yako, na watoto wetu wauone ukuu enzi yako. 17 Na neema ya Bwana Mungu wetu
iwe yetu; fanikisha kazi za mikono yetu; hakika, fanikisha kazi ya mikono yetu.

# 91

1 Yeye aishiye katika makazi ya Aliye Juu atakaa katika uvuli wa mwenyezi. 2 Nami
nitasema kuhusu Yahwe, "Yeye ni kimbilio langu na ngome yangu, Mungu wangu,
ambaye niaamini katika yeye." 3 Kwa maana yeye atakuokoa dhidi ya mtego wa
mwindaji na dhidi ya pigo liletalo mauti. 4 Yeye atakufunika kwa mbawa zake, na
chini ya mbawa zake utapata kimbilio. Uaminifu wake ni ngao na ulinzi. 5 Nawe
hautaogopeshwa na vitisho wakati wa usiku, wala mishale ipaayo kwa siku, 6 wala
pigo lizungukalo gizani, wala ugonjwa ujao wakati wa mchana. 7 Maelfu waweza

kuangukia upande wako na makumi elfu mkono wako wa kuume, lakini uovu
hauwezi kukupata. 8 Wewe utatazama tu na kuona hukumu ya waovu. 9 Kwa kuwa
Yahwe ni kimbilio langu! Umfanye Aliye Juu kuwa kimbilio lako pia. 10 Hakuna
uovu utakao kushinda wewe; mateso hayatakuja karibu na nyumba yako. 11 Maana
yeye atawaelekeza malaika moja kwa moja kukulinda wewe, na kukuwekea ulinzi
katika njia zako zote. 12 Nao watakuinua juu kwa mikono yao ili usiweze kujigonga
mguu wako kwenye jiwe. 13 Utawaangamiza simba na nyoka chini ya miguu yako;
utawakanyaga wana-simba na nyoka. 14 Kwa sababu amejitoa kwangu, nitamuokoa.
Nitamlinda kwa sababu yeye ni mwaminifu kwangu. 15 Aniitapo, nitamjibu. Katika
shida nitakuwa naye; nitampatia ushindi na nitamuheshimu. 16 Nitamtosheleza kwa
maisha malefu na kumuonesha wokovu wangu.

# 92

Zaburi, wimbo kwa ajili ya siku ya Sabato. 1 Ni jambo jema kumshukuru Yahwe
na kuliimbia sifa jina lako, Uliye Juu, 2 kutangaza uaminifu wa agano lako wakati
wa asubuhi na uaminifu wako kila usiku, 3 kwa kinubi cha nyuzi kumi na kwa tuni
ya kinubi. 4 Kwa kuwa wewe, Yahwe, matendo yako yamenifurahisha. Nitaimba
kwa furaha kwa sababu ya matendo ya mikono yako. 5 Ni jinsi gani matendo
yako ni makuu, Yahwe! mawazo yako ni ya kina. 6 Mtu mpumbavu hawezi
kuyajua, wala mjinga kuyaelewa haya: 7 Wasio haki watakapochipuka kama nyasi,
na hata watendao uovu watakapo stawi, bado wataangamizwa kwenye uharibifu
wa milele. 8 Lakini wewe, Yahwe, utatawala milele. 9 Hakika, watazame adui zako,
Yahwe! Hakika, watazame adui zako. Wataangamia! Wale wote watendao maovu
watatawanywa. 10 Wewe umeyainua mapembe yangu kama mapembe ya Nyati
wa porini; nimepakwa mafuta safi. 11 Macho yangu yameona kuanguka kwa adui
zangu; masikio yangu yamesikia maangamizi ya maadui zangu waovu. 12 Wenye haki
watastawi kama mtende; watakua kama mwerezi wa Lebanoni. 13 Wamepandwa
katika nyumba ya Yahwe; wakistawi katika nyua za Mungu wetu. 14 Wao huzaa
matunda hata uzeeni; hukaa safi na wenye afya, 15 kutangaza kuwa Yahwe ni wa
haki. Yeye ni mwamba wangu, na hakuna udhalimu ndani yake.

# 93

1 Yahwe anatawala; amevikwa adhama; Yahwe amejivika na kujifunga nguvu.
Ulimwengu umeimalishwa; hauwezi kusogezwa. 2 Kiti chako cha enzi kimeimar-
ishwa nyakati za kale; umekuwepo siku zote. 3 Bahari zimeinuka, Yahwe;
zimememepaza sauti zao; mawimbi ya bahari yapiga ghasia na ngurumo. 4 Zaidi ya
ghasia ya mawimbi mengi, mawimbi ya bahari yenye nguvu, Yahwe aliye juu ni
mwenye nguvu. 5 Amri zako makini ni za kuaminika sana; utakatifu huipamba
nyumba yako, Yahwe, milele.

# 94

1 Yahwe, Ee Mungu ulipaye kisasi, Mungu ulipaye kisasi, utuangazie sisi. 2 Inuka,
muhukumu wa nchi, uwape wenye majivuno kile wanachosahili. 3 Mpaka lini waovu,
Yahwe, mpaka lini waovu watafurahia? 4 Wanamwaga maneno yao ya kiburi; wote
watendao uovu wanajivuna. 5 Wanawaangamiza watu wako, Yahwe; wanalitesa
taifa ambao ni milki yako. 6 Wanamuua mjane na mgeni aishiye nchini mwao,
na wanamuua yatima. 7 Nao husema, “Yahwe hawezi kuona, Mungu wa Yakobo
hayagundui haya.” 8 Tambueni, ninyi watu wajinga! Enyi wapumbavu, mtajifunza
lini? 9 Yeye aliye liumba sikio, hasikii? Yeye aliye litengeneza jicho, haoni? 10 Yeye
awaadhibuye mataifa, hayuko sahihi? Yeye ndiye ampaye maarifa mwanadamu.

[11] Yahwe anayajua mawazo ya wanadamu, kuwa ni mvuke. [12] Amebarikiwa yule
ambaye umuongozaye, Yahwe, yule ambaye wewe humfundisha kutoka katika sheria
yako. [13] Wewe humpa pumziko wakati wa shida mpaka shimo litakapokuwa
limechimbwa kwa ajili ya waovu. [14] Maana Yahwe hatawaacha watu wake wala
kutelekeza warithi wake. [15] Kwa kuwa tena hukumu itakuwa ya haki; na wote
walio wanyoofu wa moyo wataifuata. [16] Ni nani atainuka kunitetea dhidi ya
watendao uovu? Ni nani atasimama dhidi ya waovu kwa ajili yangu? [17] Kama
Yahwe asingelikuwa msaada wangu, haraka ningekuwa nimelala mahali pa ukimya.
[18] Niliposema, mguu wangu unateleza," Uaminifu wa agano lako, Yahwe, uliniinua.
[19] Wasiwasi uwapo mwingi ndani yangu, faraja yako hunifurahisha. [20] Kiti cha
uharibifu chaweza kushirikiana nawe, kitungacho madhara kwa njia ya sheria?
[21] Wao kwa pamoja hupanga njama kuwaua wenye haki na kuwahukumu adhabu ya
kifo wenye haki. [22] Lakini Yahwe amekuwa mnara wangu mrefu, na Mungu wangu
amekuwa mwamba wa kimbilio langu. [23] Yeye atawarudishia uovu wao wenyewe na
atawaangamiza katika uovu wao wenyewe. Yahwe Mungu wetu atawaangamiza.

# 95

[1] Oh njoni, tumwimbie Yahwe; na tumwimbie kwa shangwe mwamba wa wokovu
wetu. [2] Tuingie uweponi mwake kwa shukrani; tumwimbie yeye kwa zaburi ya sifa.
[3] Kwa maana Yahwe ni Mungu mkuu na Mfalme mkuu juu ya miungu yote. [4] Mkononi
mwake zimo bonde za dunia; navyo vilele vya milima ni vyake. [5] Bahari ni yake,
maana aliiumba, na mikono yake ilitengeneza nchi kavu. [6] Oh njoni, tumwabudu na
tupige magoti; tupige magoti mbele za Yahwe, muumbaji wetu: [7] Kwa maana yeye ni
Mungu wetu, na sisi tu watu wa malisho yake na kondoo wa mkono wake. Ni heri
leo mngesikia sauti yake! [8] Msiifanye migumu mioyo yenu, kama vile huko Meriba,
au kama ile siku ya Masa jangwani, [9] ambako baba zenu walinijaribu na kunipima,
japo walikuwa wameyaona matendo yangu. [10] Kwa miaka arobaini nilikasirishwa na
kizazi hicho na kusema, 'Hawa ni watu ambao mioyo yao imepotoka; hawazijui njia
zangu.' [11] Hivyo katika hasira yangu niliapa kwamba wasingeingia kamwe mahali
pa pumziko."

# 96

[1] Oh, mwimbieni Yahwe wimbo mpya; mwimbieni Yahwe, nchi yote. [2] Mwimbieni
Yahwe, tukuzeni jina lake; tangazeni wokovu wake siku hadi siku. [3] Tangazeni
utukufu wake kati ya mataifa, matendo yake ya ajabu kati ya mataifa. [4] Maana
Yahwe ni mkuu na wakusifiwa sana. Ni wakuhofiwa kuliko miungu mingine. [5] Maana
miungu yote ya mataifa ni sanamu, bali ni Yahwe aliye zifanya mbingu. [6] Heshima
na adhama ziko mbele zake. Nguvu na uzuri zimo katika patakatifu pake. [7] Mpeni
Yahwe sifa, enyi ukoo wa watu, mpeni sifa Yahwe kwa ajili ya utukufu wake na nguvu.
[8] Mpeni Yahwe utukufu ambao unastahili jina lake. Leteni matoleo na muingie nyuani
mwake. [9] Mpigieni magoti Yahwe mkiwa mmevaa mavazi ambayo yanaheshimu
utakatifu wake. Nchi yote tetemekeni mbele zake. [10] Semeni kati ya mataifa, Yahwe
anatawala." Ulimwengu pia umeimarishwa; hauwezi kutikiswa. Yeye huwahukumu
watu kwa haki. [11] Mbingu na zifurahi, na nchi ishangilie; bahari na ivume na vyote
viijazavyo vipige kelele kwa shangwe. [12] Mashamba yashangilie na vyote vilivyomo.
Kisha miti ya mstuni ipige kelele kwa furaha [13] mbele za Yahwe, maana yeye anakuja.
Anakuja kuihukumu nchi. Naye atauhukumu ulumwengu kwa haki na mataifa kwa
uaminifu wake.

# 97

1 Yahwe anatawala; nchi ishangilie; visiwa vingi na vifurahi. 2 Mawingu na giza
vyamzunguka. Haki na hukumu ndio msingi wa kiti chake. 3 Moto huenda mbele
zake nao huwateketeza adui zake pande zote. 4 Taa yake huangaza ulimwengu; nchi
huona na kutetemeka. 5 Milima huyeyuka kama nta mbele za Yahwe, Bwana wa
dunia yote. 6 Mbingu hutangaza haki yake, na mataifa yote huuona utukufu wake.
7 Wale wote waabuduo sanamu za kuchonga wataaibishwa, wale wanao jivuna katika
sanamu zisizo na maana mpigieni yeye magoti, enyi miungu wote! 8 Sayuni ilisikia na
kufurahi, na miji ya Yuda ilishangilia kwa sababu ya amri zako za haki, Yahwe. 9 Kwa
kuwa wewe, Yahwe, ndiye uliye juu sana, juu ya nchi yote. Umetukuka sana juu ya
miungu yote. 10 Ninyi ambao mnampenda Yahwe, chukieni uovu! Yeye hulinda uhai
wa watakatifu wake, naye huwatoa mikononi mwa waovu. 11 Nuru imepandwa kwa
ajili ya wenye haki na furaha kwa ajili ya wanyoofu wa moyo. 12 Furahini katika
Yahwe, enyi wenye haki; na mpeni shukurani mkumbukapo utakatifu wake.

# 98

Zaburi. 1 Oh, mwimbieni Yahwe wimbo mpya, kwa kuwa ametenda mambo ya
ajabu; mkono wake wa kuume na mkono wake mtakatifu vimempa ushindi. 2 Yahwe
ameufanya wokovu wake ujulikane; ameidhihirisha haki yake kwa mataifa yote.
3 Hukumbuka uaminifu wa agano lake na uaminifu kwa ajili ya nyumba ya Israeli;
miisho yote ya dunia itauona ushindi wa Mungu wetu. 4 Mshangilieni Yahwe, nchi
yote; pazeni sauti kwa wimbo, imbeni kwa furaha, na imbeni sifa. 5 Mwimbieni
Yahwe sifa kwa kinubi, kwa kinubi na wimbo wenye muiki wa kupendeza. 6 Kwa
panda na sauti ya baragumu, fanyeni kelele za shangwe mbele ya Mfalme, Yahwe.
7 Bahari na ipige kelele na vyote vilivyomo, ulimwengu na wale wakaao ndani
yake! 8 Mito na ipige makofi, na milima ipige kelele kwa furaha. 9 Yahwe anakuja
kuihukumu nchi; naye ataihukumu dunia kwa haki na mataifa kwa adili.

# 99

1 Yahwe anatawala; mataifa na yatetemeke. Ameketi juu ya makerubi; nchi
inatetemeka. 2 Yahwe ni mkuu katika Sayuni; naye ametukuka juu ya mataifa yote.
3 Nao walisifu jina lako kuu na lenye kutisha; yeye ni mtakatifu. 4 Mfalme ana nguvu,
naye hupenda haki. Wewe umeimarisha haki; umetenda haki na hukumu katika
Yakobo. 5 Msifuni Yahwe Mungu wetu na sujuduni miguuni pake. Yeye ni mtakatifu.
6 Musa na Haruni walikuwa miongoni mwa makuhani wake, na Samweli alikuwa
miongoni mwa wale walio muomba Yeye. Walimuomba Yahwe, naye akawajibu.
7 Alizungumza nao toka nguzo ya wingu. Walizishika amri zake takatifu na sheria
ambazo aliwapatia. 8 Wewe uliwajibu, Yahwe Mungu wetu. Ulikuwa kwao Mungu
mwenye kusamehe, lakini uliye adhibu matendo yao ya dhambi. 9 Msifuni Yahwe
Mungu wetu, na mwabuduni kwenye mlima wake mtakatifu, maana Yahwe Mungu
wetu ni Mtakatifu.

# 100

Zaburi ya shukrani. 1 Mpigieni Yahwe kelele za furaha, enyi nchi yote. 2 Mtumikieni
Yahwe kwa furaha; njoni mbele zake mkiimba kwa furaha. 3 Mjue kuwa Yahwe
ni Mungu; alituumba, na sisi tu wake. Tu watu wake na kondoo wa malisho yake.
4 Ingieni malangoni mwake kwa shukrani na nyuani mwake kwa kusifu. Mshukuruni
yeye na litukuzeni jina lake. 5 Maana Yahwe ni mwema; uaminifu wa agano lake
wadumu milele na uaminifu wake vizazi na vizazi vyote.

# 101

Zaburi ya Daudi. [1] Nitaimba uaminifu wa agano lako na hukumu; kwako, Ee Yahwe,
Nitakuimbia sifa. [2] Nitatembea katika njia ya uadilifu. Oh, ni lini utakuja kwangu?
Nitatembea kwa uadilifu ndani ya nyumba yangu. [3] Sitaweka matendo maovu mbele
ya macho yangu; ninachukia uovu usio na maana; hauta shikamana nami. [4] Watu
waliopotoka wataniacha mimi; mimi sichangamani na uovu. [5] Nitamwangamiza
yeyote amsengenyaye jirani yake kwa siri. Sitamvumilia yeyote mwenye kiburi.
[6] Nitawachagua walio waaminifu katika nchi wakae upande wangu. Wale watembeao
katika njia ya uhadilifu watanitumikia. [7] Watu wadanganyifu hawatabaki ndani ya
nyumba yangu; waongo hawatakaribishwa mbele ya macho yangu. [8] Asubuhi hata
asubuhi nitawaangamiza waovu wote kutoka nchini; nitawaondoa watendao maovu
wote katika mji wa Yahwe.

# 102

Maombi ya aliyeteswa wakati yeye alipolemewa na kumwaga maombolezo yake
mbele ya Yahwe. [1] Sikia maombi yangu, Ee Yahwe; sikia kulia kwangu kwako.
[2] Usiufiche uso wako mbali nami wakati wa shida. Unisikilize. Nikuitapo, unijibu
upesi. [3] Kwa maana siku zangu zinapita kama moshi, na mifupa yangu kama
moto. [4] Moyo wangu umeumizwa na niko kama majani yaliyo kauka. Ninasahau
kula chakula chochote. [5] Kwa muendelezo wa kuugua kwangu, nimekonda sana.
[6] Niko kama mwali wa jangwani; nimekuwa kama bundi magofuni. [7] Ninalala
macho kama shomoro faraghani, pekeyake juu ya paa. [8] Adui zangu wananilaumu
mchana kutwa; wale wanao nidhihaki hutumia jina langu katika laana. [9] Ninakula
majivu kama mkate na kuchanganya kinywaji changu kwa machozi. [10] Kwa sababu
ya hasira yako kali, umeniinua juu kunitupa chini. [11] Siku zangu ni kama kivuli
kanachofifia, na ninanyauka kama majani. [12] Lakini wewe, Yahwe, unaishi milele,
na kumbukumbu lako ni kwa vizazi vyote. [13] Wewe utasimama na kuirehemu
Sayuni. Sasa ni wakati wa mkurehemu yeye. Wakati ulio teuliwa umefika. [14] Maana
watumishi wako wameyaridhia mawe yake pendwa na kuyaonea huruma mavumbi
ya magofu yake. [15] Mataifa wataliheshimu jina lako, Yahwe, na wafalme wote wa
nchi watauheshimu utukufu wako. [16] Yahwe ataijenga tena Sayuni na ataonekana
katika utukufu wake. [17] Wakati huo, atajibu maombi ya fukara; hatayakataa maombi
yao. [18] Hii itaandikwa kwa ajili ya vizazi vijavyo, na watu ambao bado hawajazaliwa
watamsifu Yahwe. [19] Maana ametazama chini toka mahali pa juu patakatifu; [20] Toka
mbinguni Yahwe ameiangalia nchi, ili kusikia kuugua kwa wafungwa, kuwafungua
waliohukumiwa kufa. [21] Kisha watu watalitangaza jina la Yahwe katika Sayuni na
sifa zake katika Yerusalemu [22] pindi mataifa na falme watakapokusanyika pamoja
kumtumikia Yahwe. [23] Amechukua nguvu zangu katikati ya siku zangu za kuishi,
amezifupisha siku zangu. [24] Nilisema, “Mungu wangu, usinichukue katikati ya siku
zangu; wewe uko hapa hata kizazi chote. [25] Tangu zama za kale wewe uliiweka nchi
mahali pake; mbingu ni kazi ya mikono yako. [26] Mbingu na nchi zitaangamia lakini
wewe utabaki; zitachakaa kama mavazi; utaziondoa kama watu waondoavyo mavazi
yaliyo chakaa, nazo hazitaonekana tena. [27] Lakini wewe ni yuleyule, na miaka yako
haitakuwa na mwisho. [28] Watoto wa watumishi wako wataendelea kuishi, na uzao
wao utaishi katika uwepo wako.

# 103

Zaburi ya Daudi. [1] Nitamsifu Yahwe maisha yangu yote, na vyote vilivyomo ndani
yangu, nitalisifu jina lake takatifu. [2] Maishani mwangu mwote nitamsifu Yahwe,
na kukumbuka matendo yake yote mazuri. [3] Yeye husamehe dhambi zako zote;

huponya magonjwa yako yote. 4 Huukomboa uhai wako dhidi ya uharubifu; hukuvika
taji kwa uaminifu wa agano lake na hutenda kwa rehema. 5 Huyatosheleza maisha
yako kwa mambo mema ili kwamba ujana wako ufanywe upya kama tai. 6 Yahwe
hutenda yaliyo haki naye hutenda hukumu ya haki kwa ajili ya wote walio onewa.
7 Alimjulisha Musa njia zake, matendo yake kwa uzao wa Israeli. 8 Yahwe ni wa
huruma na neema; ni mvumilivu; ana agano kuu la uaminifu. 9 Hataadhibu siku
zote; hakasiriki siku zote. 10 Hatushughulikii sisi kama dhambi zetu zinavyostahili
au kutulipa kulingana na uhitaji wa dhambi zetu. 11 Kama mbingu zilivyo juu zaidi
ya nchi, ndivyo ulivyo ukuu wa uaminifu wa agano lake kwao wale wanaomcha
yeye. 12 Kama vile mashariki ilivyo mbali na magharibi, hivi ndivyo ameondoa hatia
zetu za dhambi zetu mbali nasi. 13 Kama vile baba alivyo na huruma kwa watoto
wake, ndivyo Yahwe alivyo na huruma kwao wamchao. 14 Maana anajua tulivyo
umbwa; anajua kuwa tu mavumbi. 15 Kama ilivyo kwa mwanadamu, siku zake ni
kama majani; hustawi kama ua katika shamba. 16 Upepo hulipiga, nalo hutoweka, na
hakuna hata mmoja awezaye kuelezea mahali lilipokua. 17 Lakini agano la uaminifu
wa Yahwe uko kwa wale wamchao yeye milele hata milele. Haki yake ni endelevu
kwa uzao wao. 18 Wanashika agano lake na kukumbuka kutii maagizo yake. 19 Yahwe
ameweka kiti chake cha enzi mbinguni, na ufalme wake watawala juu ya kila mtu.
20 Msifuni Yahwe, enyi malaika zake, ninyi hodari wenye nguvu na mtendao neno
lake, na kutii sauti ya neno lake. 21 Msifuni Yahwe, enyi jeshi la malaika wote, ninyi
ni watumishi mfanyao mapenzi yake. 22 Msifuni Yahwe, viumbe wake wote, mahali
popote atawalapo. Nitamsifu Yahwe maisha yangu yote.

# 104

1 Nitamsifu Yahwe maisha yangu yote, Ewe Yahwe Mungu wangu, wewe ni mkubwa
sana; umevikwa kwa utukufu na enzi. 2 Unajifunika mwenyewe kwa nuru kama kwa
mavazi; umetandaza mbingu kama pazia za hema. 3 Umeweka mawinguni mihimili
ya vyumba vyako; huyafanya mawingu gari lako; hutembea juu ya mbawa za upepo.
4 Yeye huufanya upepo kuwa wajumbe wake, miale ya moto kuwa watumishi wake.
5 Aliiweka misingi ya nchi, nayo haitahamishwa kamwe. 6 Wewe uliifunika nchi kwa
maji kama kwa mavazi; maji yalifunika milima. 7 Kukemea kwako kulifanya maji
kupungua; kwa sauti ya radi yako yakaondoka kasi. 8 Milima iliinuka, na mabonde
yakaenea mahali ambapo wewe ulikwisha pachagua kwa ajili yao. 9 Umeweka
mipaka kwa ajili yao ambao hayawezi kuupita; hayawezi kuifunika nchi tena. 10 Yeye
alifanya chemchemi kutiririsha maji mabondeni; mito kutiririka katikati ya milima.
11 Inasambaza maji kwa ajili ya wanyama wote wa shambani; punda wa porini
hukata kiu yao. 12 Kandokando ya mito ndege hujenga viota vyao; huimba kati ya
matawi. 13 Humwagilia milima kutoka katika chumba chake cha maji mawinguni.
Nchi imejazwa kwa matunda ya kazi yake. 14 Huzifanya nyasi kukua kwa ajili ya
mifugo na mimea kwa ajili ya binadamu kulima ili kwamba mwanadamu aweze
kuzalisha chakula toka nchini. 15 Hutengeneza mvinyo kumfurahisha mwanadamu,
mafuta yakumfanya uso wake ung'ae, na chakula kwa ajili ya kuimarisha uhai wake.
16 Miti ya Yahwe hupata mvua nyingi; Mierezi ya Lebanoni aliyoipanda. 17 Hapo
ndege hutengeneza viota vyao. Na korongo, misunobari ni nyuma yake. 18 Mbuzi
mwitu huishi kwenye milima mrefu; na urefu wa milima ni kimilio la wibari.
19 Aliuchagua mwezi kuweka alama ya majira; jua latambua kuchwa kwake. 20 Wewe
hufanya giza la usiku ambapo wanyama wote wa msituni hutoka nje. 21 Wana simba
huunguruma kwa ajili ya mawindo na hutafuta chakula chao kutoka kwa Mungu.
22 Jua linapochomoza, huenda zao na kujilaza mapangoni mwao. 23 Wakati huo huo,
watu hutoka nje kuelekea kazi zao na utumishi wake mpaka jioni. 24 Yahwe, ni jinsi

gani kazi zako zilivyo nyingi na za aina mbalimbali! Kwa hekima ulizifanya zote;
nchi inafurika kwa kazi zako. 25 Kule kuna bahari, yenye kina kirefu na pana, ikiwa
na viume vingi visivyo hesabika, vyote vidogo na vikubwa. 26 Meli husafili humo, na
ndimo alimo Lewiathani uliye muumba acheze baharini. 27 Hawa wote hukutazama
wewe uwape chakula kwa wakati. 28 Unapowapa chakula, hukusanyika; ufunguapo
mkono wako, wanatosheka. 29 Unapouficha uso wako, wanateseka; ukiiondoa pumzi
yao, wanakufa na kurudi mavumbini. 30 Unapotuma Roho yako, wanaumbwa, nawe
unaifanya upya nchi. 31 Utukufu wa Yahwe na udumu milele; Yahwe na aufurahie
uumbaji wake. 32 Yeye hutazama nchi, nayo hutikisika; huigusa milima, nayo hutoa
moshi. 33 Nitamwimbia Yahwe maisha yangu yote; nitamwimbia sifa Mungu wangu
nigali ninaishi. 34 Mawazo yangu na yawe matamu kwake; nitafurahia katika Yahwe.
35 Wenye dhambi na waondoshwe katika nchi, na waovu wasiwepo tena. Ninamsifu
Yahwe maisha yangu yote. Msifuni Yahwe.

# 105

1 Mshukuruni Yahwe, liitieni jina lake; myafanye matendo yake yajulikane kati
ya mataifa. 2 Mwimbieni yeye, mwimbieni sifa yeye; semeni matendo yake yote ya
ajau. 3 Mjivune katika utakatifu wa jina lake; moyo wao wamtafutao Yahwe ufurahi.
4 Mtafuteni Yahwe na nguvu zake; utafuteni uwepo wake siku zote. 5 Kumbukeni
mambo ya ajabu aliyoyatenda, 6 miujiza yake na amri zitokazo kinywani mwake,
enyi kizazi cha Ibrahimu mtumishi wake, enyi watu wa Yakobo, wachaguliwa wake.
7 Yeye ni Yahwe, Mungu wetu. Amri zake ziko juu ya nchi yote. 8 Naye hulikumbuka
agano lake milele, neno alilo amuru kwa ajili ya vizazi elfu. 9 Hulikumbuka agano
alilolifanya na Ibrahimu na kiapo alicho mwapia Isaka. 10 Hiki ndicho alicho
mthibitishia Yakobo kama agano na kama agano la milele kwa Israeli. 11 Alisema,
“Nitakupa wewe ardhi ya Kanaani kama sehemu yako ya urithi.” 12 Alisema hili
wakati tu walipokuwa wachache katika hesabu, yaani wachahe sana, nao walikuwa
wageni katika nchi. 13 Walienda taifa hadi taifa na kutoka ufalme moja kwenda
mwingine. 14 Hakuruhusu yeyote kuwaonea; aliwakemea wafalme kwa ajili yao.
15 Alisema, “Msiwaguze wapakwa mafuta wangu, na msiwadhuru manabii wangu.”
16 Aliita njaa katika nchi; akaondoa upatikanaji wa mkate wote. 17 Akatuma mtu
mbele yao; Yusufu aliuzwa kama mtumishi. 18 Miguu yake ilifungwa kwa pingu;
alivishwa mnyororo wa chuma shingoni mwake, 19 mpaka wakati wa maneno yake
ulipotimia, nalo neno la Yahwe lilimjaribu. 20 Mfalme alituma watumishi kumfungua;
mtawala wa watu alimuweka huru. 21 Alimuweka kuwa msimamizi wa nyumba
yake kama mtawala wa mali zake zote 22 kuwaelekeza wakuu kama alivyopenda
na kuwafundisha viongozi wake hekima. 23 Kisha Israeli iliingia Misri, na Yakobo
aliishi kwa muda katika nchi ya Hamu. 24 Yahwe aliwajalia watu wake wazae sana,
na aliwafanya wenye nguvu kuliko adui zao. 25 Alisababisha adui zao wawachukie
watu wake, na kuwatendea visivyo watumishi wake. 26 Alimtuma Musa, mtumishi
wake, na Haruni, ambaye alikwisha mchagua. 27 Walifanya ishara zake kati ya
Wamisri na maajabu yake katika ya nchi ya Hamu. 28 Alituma giza na likaifanya
nchi hiyo kuwa giza, lakini watu wake hawakutii amri zake. 29 Aligeuza maji kuwa
damu na aliua samaki wao. 30 Nchi yao ilijaa vyura, hata katika vyumba vya
watawala wao. 31 Alisema, na makundi ya inzi na chawa wakaja mjini mwote.
32 Aliigeuza mvua yao kuwa mvua ya mawe, pamoja na miali ya moto juu ya
ardhi yao. 33 Aliiharibu mizabibu yao na mitini yao; akaivunja miti ya mji wao.
34 Alisema, na nzige wakaja, nzige wengi sana. 35 Nzige walikula mboga zao zote
za majani katika nchi yao. Walikula mazao yote ardhini. 36 Aliua kila mzaliwa

wa kwanza katika nchi yao, malimbuko ya nguvu zao. 37 Aliwatoa nje Waisraeli
wakiwa na fedha na dhahabu; hakuna mmoja wa kabila lake aliyejikwaa njiani.
38 Misri ilifurahi walipoondoka, maana Wamisri waliwaogopa. 39 Alitandaza wingu
liwafunike na alifanya moto uwaangazie wakati wa usiku. 40 Waisraeli waliomba
chakula, naye aliwaletea kware na aliwatosheleza kwa mkate kutoka mbiguni.
41 Aliugawa mwamba, maji yalimwagika kutoka humo; yalitiririka katika jangwa
kama mto. 42 Kwa maana alikumbuka ahadi yake takatifu aliyoifanya kwa Ibrahimu
mtumishi wake. 43 Aliwaongoza watu wake kwa furaha, wateule wake kwa kelele za
ushindi. 44 Aliwapa nchi za mataifa; walichukua milki ya mali za watu 45 ili waweze
kushika amri zake na kutii sheria zake. Msifuni Yahwe.

# 106

1 Msifuni Yahwe. Mshukuruni Yahwe, kwa kuwa ni mwema, kwa maana uaminifu
wa agano lake wadumu milele. 2 Ni nani awezaye kuyahesabu mataendo makuu
ya yahwe au kutangaza katika ukamilifu sifa zote za matendo yake ya kuaminika.
3 Wamebarikiwa wale watendao yaliyo mema na matendo yao yaliyo haki siku zote.
4 Ukumbuke, Ee Yahwe, unapowaonesha watu wako neema; unisaidie unapowaokoa.
5 Ndipo nitaona mafanikio ya wateule wako, wakifurahia katika furaha ya taifa
lako, na utukufu pamoja na urithi wako. 6 Tumefanya dhambi kama babu zetu,
tumekosea, na kufanya uovu. 7 Baba zetu hawakuyatambua matendo yako ya
ajabu katika Misri; walipuuzia matendo yako mengi ya uaminifu wa agano; waliasi
penye bahari, bahari ya Shamu. 8 Hata hivyo, yeye aliwaokoa kwa ajili ya jina
lake ili kwamba aweze kuzifunua nguvu zake. 9 Aliikemea Bahari ya Shamu, nayo
ikakauka. Kisha akawaongoza vilindini, kana kwamba ni jangwani. 10 Aliwaokoa
kutoka mkononi mwa wale waliowachukia, na aliwaokoa kutoka mkononi mwa
adui. 11 Lakini maji yaliwafunika washindani wao; hakuna hata mmoja aliye
okolewa. 12 Ndipo waliyaamini maneno yake, nao waliimba sifa zake. 13 Lakini
walisahau haraka kile alichofanya; hawakuyasubiri maelekezo yake. 14 Walikuwa
na tamaa isiyotoshelezwa jangwani, wakamjaribu Mungu nyikani. 15 Aliwapa ombi
lao, lakini alituma gonjwa ambalo lilishambulia miili yao. 16 Katika kambi wakawa
na wivu juu Musa na Haruni, kuhani mtakatifu wa Yahwe. 17 Nchi ilifunguka na
ilimmeza Dathani na iliwafunika wafuasi wa Abiramu. 18 Moto uliwaka kati yao;
moto uliwaangamiza waovu. 19 Walitengeneza ndama huko Horebu na kuabudu
sanamu ya kuyeyuka. 20 Wakaubadili utukufu wa Mungu kuwa mfano wa ng'ombe
alaye majani. 21 Walimsahau Mungu wokozi wao, aliyefanya mambo makuu katika
Misri. 22 Alifanya matendo ya ajabu katika nchi ya Hamu na matendo makuu
penye Bahari ya Shamu. 23 Mungu angetangaza uharibifu wao, kama sio Musa,
mteule wake, aliingilia kati kugeuza hasira yake dhidi ya kuwaangamiza. 24 Kisha
waliidharau nchi yenye matunda; hawakuiamini ahadi yake, 25 bali walilalamiaka
katika mahema yao, na hawakumtii Yahwe. 26 Kwa hiyo aliinua mkono wake na
kuapa kwao kuwa atawaacha wafe jangwani, 27 akitawanya uzao wao kati ya mataifa,
na kuwatawanya katika nchi za kigeni. 28 Waliabudu Baal ya Poeri na walizila
dhabihu zilizotolewa kwa wafu. 29 Walimkasirisha kwa matendo yao, na pigo la
gonjwa baya liliwashambulia kati yao. 30 Ndipo Finehasi aliinuka kuingilia kati,
na pigo likakoma. 31 Ilihesabika kwake kama tendo la haki kwa vizazi vyote hata
milele. 32 Pia walimkasirisha Yahwe penye maji ya Meriba, na Musa aliteseka kwa ajili
yao. 33 Walimghadhabisha Musa naye akaongea haraka. 34 Hawakuyaharibu mataifa
kama Yahwe alivyowaamuru, 35 bali walichangamana na mataifa na walijifunza njia
zao 36 nao waliabudu sanamu, nazo zikawa mtego kwao. 37 Waliwatoa wana wao na
binti zao kwa mapepo. 38 Walimwaga damu isiyo na hatia, damu ya wana na binti zao,

ambao waliwatoa kama dhabihu kwa sanamu za Kanaani, waliinajisi nchi kwa damu.
39 Walinajisiwa kwa matendo yao; katika matendo yao walikuwa kama malaya.
40 Hivyo Yahwe aliwakasilikia watu wake, akawadharau watu wake mwenyewe.
41 Akawaruhusu mataifa, na wale walio wachukia wakawatawala. 42 Maadui zao
wakawaonea, wakatiishwa chini ya mamlaka yao. 43 Mara nyingi alienda kuwasaidia,
lakini waliendelea kuasi nao walishushwa chini kwa dhambi zao wenyewe. 44 Hata
hivyo, aliiangalia dhiki yao aliposikia kilio chao kwa ajili ya msaada. 45 Alikumbuka
agano lake pamoja nao na alijirudi kwa sababu ya upendo wake thabiti. 46 Aliwafanya
wote waliowateka wawahurumie. 47 Utuokoe, Ee Yahwe, Mungu wetu. Utukusanye
kutoka kati ya mataifa ili kwamba tuweze kulishukuru jina lako takatifu na utukufu
katika sifa zako. Yahwe, 48 Mungu wa Israeli, na asifiwe toka milele na milele. watu
wote walisema, “Amen.” Msifuni Yahwe. Kitabu cha tano.

# 107

1 Mshukuruni Yahwe, maana ni mwema, na uaminifu wa agano lake wadumu
milele. 2 Waseme hivi waliokombolewa na Yahwe, wale aliowaokoa toka mkononi
mwa adui. 3 Yeye amewakusanya kutoka nchi za kigeni, kutoka mashariki na
magharibi, kutoka kaskazini na kusini. 4 Walitanga-tanga janwani katika njia ya nyika
hawakuona mji wa kuishi. 5 Kwa sababu walikuwa na njaa na kiu, walikata tamaa
kutokana na uchovu. 6 Kisha walimuita Yahwe katika shida yao, naye aliwaokoa toka
katika dhiki yao. 7 Aliwaongoza kupitia njia ya moja kwa moja waweze kwenda mjini
kuishi humo. 8 Oh ili watu wamsifu Yahwe kwa ajili ya uaminifu wa agano lake
na kwa mambo ya ajabu aliowatendea wanadamu! 9 Maana hutosheleza shauku
za walio na kiu, na hamu ya wale wenye njaa yeye huwashibisha kwa mambo
mema. 10 Baadhi walikaa katika giza na uvuli wa mauti, walifungwa katika mateso na
minyororo. 11 Hii ni kwa sababu walikuwa wameliasi neno la Mungu na walikataa
maelekezo ya Aliye Juu. 12 Aliinyenyekesha mioyo yao kupitia magumu; walipata
mashaka na hakukuwa na mmoja wa kuwasaidia. 13 Kisha wakamwita Yahwe katika
shida yao, naye akawatoa katika dhiki yao. 14 Aliwatoa gizani na kwenye uvuli wa
mauti na kuvunja vifungo vyao. 15 Oh ili watu wamsifu Yahwe kwa ajili ya uaminifu
wa agano lake na kwa mambo ya ajabu aliyoyatenda kwa wanadamu! 16 Kwa maana
amevunja malango ya shaba na kukata mapingo ya chuma. 17 Walikuwa wapumbavu
katika njia zao za uasi na kuteswa kwa sababu ya dhambi zao. 18 Walipoteza hamu
yao ya kula chakula chochote, na waliyakaribia malango ya kifo. 19 Kisha walimlilia
Yahwe katika shida yao, naye akawatoa katika dhiki yao. 20 Alituma neno lake na
likawaponya, na akawaokoa kutoka katika uharibifu wao. 21 Oh ili watu wamsifu
Yahwe kwa ajili ya uaminifu wa agano lake na kwa mambo ya ajabu aliyoyatenda
kwa wanadamu! 22 Na watoe dhabihu ya shukrani na kutangaza matendo yake
kwa kuimba. 23 Baadhi husafiri baharini katika meli na kufanya biashara juu ya
bahari. 24 Hawa huona matendo ya Yahwe na maajabu yake baharini. 25 Kwa
maana aliamuru na alivumisha upepo wa dhoruba ambao uliyainua juu mawimbi
ya baharini. 26 Walipanda juu mawinguni na kushuka vilindini. Nafsi zao ziliyeyuka
katika dhiki. 27 Waliyumba-yumba na kupepesuka kama walevi na hawakujua la
kufanya. 28 Kisha walimlilia Yahwe katika shida yao, naye akawatoa katika dhiki yao.
29 Aliituliza dhoruba, na mawimbi yakatulia. 30 Ndipo walifurahia kwa sababu bahari
ilikuwa shwali, na aliwaleta kwenye bandari waliyoitamani. 31 Oh, ili watu wamsifu
Yahwe kwa ajili ya uaminifu wa agano lake na kwa mambo ya ajabu aliyowatendea
wanadamu! 32 Wamtukuze yeye katika kusanyiko la watu na wamsifu yeye katika
baraza la viongozi. 33 Aligeuza mito ikwa jangwa, chemchem ya maji ikawa nchi
kame, 34 na nchi ya matunda mengi ikawa nchi isiyozaa kwa sababu ya uovu wa watu

wake. 35 Aligeuza jangwa likawa ziwa la maji na nchi kame ikawa chemchem ya maji.
36 Aliwakalisha huko wenye njaa, nao walijenga mji na kuishi humo. 37 Walijenga mji
ili kupanda mimea shambani, kupanda mizabibu, na kuleta humo mazao tele. 38 Yeye
huwabariki wameongezeka sana katika hesabu. Haachi mifugo yao ipungue katika
hesabu. 39 Kisha wakapungua na kudhilika kwa dhiki na mateso. 40 Akawamwagia
viongozi dharau na akawafanya wazunguke katika jangwa, mahali pasipo na njia.
41 Lakini aliwalinda wahitaji dhidi ya mateso na kujali kwa ajili ya familia yake kama
kundi la kondoo. 42 Wenye haki wataona hili na kufurahi, na uovu wote utaona
na kufunga kinya chake. 43 Yeyote mwenye hekima anapaswa kuyaangalia haya na
kutafakari juu ya matendo ya uaminifu wa agano la Yahwe.

# 108

Wimbo, Zaburi ya Daudi. 1 Ee Mungu, moyo wangu u thabiti; nitaimba, naam,
nitaimba sifa pia kwa moyo mkuu. 2 Amka, kinanda na kinubi; nitaamka alfajiri.
3 Nitakushukuru wewe, Yahwe, kati ya watu; nitakuimbia sifa kati ya mataifa. 4 Kwa
maana uaminifu wa agano lako ni mkuu juu ya mbingu; na uaminifu wako wafika
mawinguni. 5 Ee Mungu, uinuliwe, juu ya mbingu, na utukufu wako utukuke juu
ya nchi. 6 Ili kwamba wale uwapendao waokolewe, utuokoe sisi kwa mkono wako
wa kuume na unijibu. 7 Mungu ameongea katika utakatifu wake; "Nitashangilia;
nitaigawanya Shekemu na nitalipima bonde la Sukothi. 8 Gileadi ni yangu, na manase
ni yangu; Ephraimu ni nguvu ya kichwa changu; Yuda ni fimbo yangu ya kifalme.
9 Moabu ni bakuli langu la kunawia; nitatupa kiatu changu juu ya Edomu; nitapaza
sauti katika ushindi kwa ajili ya Filisti. 10 Ni nani atakaye nipeleka kwenye mji imara?
Ni nani atakayeniongoza mpaka Edomu?" 11 Ee Mungu, sio wewe uliyetukataa?
Hauendi vitani na jeshi letu. 12 Utupe msaada dhidi ya adui yetu, maana msaada
wa wanadamu ni bure. 13 Tutashinda kwa msaada wa Mungu; atawakanyaga kwa
adui zetu.

# 109

Kwa kiongozi wa muziki. 1 Zaburi ya Daudi. Mungu ninaye msifu, usinyamaze
kimya. 2 Kwa maana waovu na wadanganyifu wananishambulia; wanazungumza
uongo dhidi yangu. 3 Wananizunguka na kusema mambo ya chuki, na wananisham-
bulia bila sababu. 4 Wananilipa kashfa badala ya upendo, lakini mimi ninawaombea.
5 Wananilipa uovu badala ya mema, na wanachukia upendo wangu. 6 Teua mtu
mwovu aliye adui zaidi kama watu hawa; teua mshitaki asimame mkono wake wa
kuume. 7 Na atakapohukumiwa, aonekane na hatia; maombi yake yachukuliwe
kuwa ni dhambi. 8 Siku zake na ziwe chahe; mamlaka yake na yachukuliwe na
mtu mwingine. 9 Watoto wake wawe yatima, na mke wake awe mjane. 10 Watoto
wake wenye kutanga tanga na kuombaomba, wakiondoka katika nyumba zao zilizo
haribika na kuomba chakula au pesa kwa wapita njia. 11 Mdai na achukue vitu
vyake vyote amilikivyo; wageni wateke mapato ya kazi yake. 12 Asiwepo mtu yeyote
wa kumfanyia wema; mtu yeyote asiwahurumie yatima wake. 13 Watoto wake
waangamizwe; majina yao na yafutwe katika kizazi kijacho. 14 Uovu wa baba zake
utajwe kwa Yahwe; na dhambi ya mama yake isisahaulike. 15 Hatia zao na ziwe
mbele ya Yahwe siku zote; Yahwe na aiondoe kumbukumbu yao duniani. 16 Yahwe
na afanye hivi kwa sababu mtu huyu kamwe hakusumbuka kuonesha uaminifu wa
agano wowote, lakini badala yake aliwasumbua wanyonge, wahitaji, na kuwaua
walio vunjika moyo. 17 Alipenda kulaani; na imrudie juu yake. Alichukia kubariki;
baraka zozote na zisije kwake. 18 Alijivika kulaani kana kwamba ni vazi lake,
na laana yake iliingia ndani yake kama maji, na kama mafuta mifupani mwake.

[19] Laana zake na ziwe kwake kama vazi avaalo kujifunika mwenyewe, na kama
mkanda avaao kila siku. [20] Na haya yawe malipo ya mshitaki wangu kutoka kwa
Yahwe, ya wale wasemao mambo maovu juu yangu. [21] Yahwe Bwana wangu,
unishughulikie kwa wema kwa ajili ya jina lako. Kwa sababu uaminifu wa agano
lako ni mwema, uniokoe. [22] Kwa maana ni mnyonge na muhitaji, na moyo wangu
umejeruhiwa ndani yangu. [23] Ninatoweka kama kivuli cha jioni; ninapeperushwa
kama nzige. [24] Magoti yangu ni dhaifu kutokana na kufunga; ninakuwa mwembamba
na mifupa. [25] Nimedharauliwa na washitaki wangu; wanionapo; hutikisa vichwa
vyao. [26] Nisaidie, Yahwe Mungu wangu; uniokoe kwa uaminifu wa agano lako. [27] Nao
wajue kuwa wewe umefanya haya, kwamba wewe, Yahwe, umetenda haya. [28] Ingawa
wananilaani, tafadhali unibariki; wanishambuliapo, waaibishwe, lakini mtumishi
wako afurahi. [29] Washitaki wangu na wavishwe kwa aibu; wavae aibu yao kama vazi.
[30] Kwa kinywa changu ninatoa shukrani kuu kwa Yahwe; nitamsifu yeye katikati ya
kusanyiko. [31] Maana nitasimama mkono wa kuume wa mhitaji, ili nimuokoe dhidi
ya wale wanao muhukumu.

# 110

Zaburi ya Daudi. [1] Yahwe humwambia bwana wangu, “Kaa mkono wangu wa
kuume mpaka nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako.” [2] Yahwe atainyosha
fimbo ya nguvu yako toka Sayuni; utawale kati ya adui zako. [3] Siku ile ya uweza wako
watu wako watakufuata wakiwa katika mavazi matakatifu ya hiari yao wenyewe;
tokea tumbo la alfajiri ujana wako utakuwa kwako kama umande. [4] Yahwe ameapa,
na hatabadilika: “Wewe ni kuhani milele, baada ya namna ya Melkizedeki.” [5] Bwana
yuko mkono wako wa kuume. Siku ile ya hasira yake atawaua wafalme. [6] Yeye
atahukumu matifa; ataujaza uwanja wa vita kwa maiti; atawauwa viongozi kaitka
nchi nyingi. [7] Atakunywa maji ya kijito njiani, kisha baada ya ushindi atainua kichwa
chake juu.

# 111

[1] Msifuni Yahwe. Nitamshukuru Yahwe kwa moyo wangu wote katikati ya
kusanyiko la wanye haki, na katika mkutano. [2] Kazi za Yahwe ni kuu, zikisubiriwa na
wale wazitamanio. [3] Kazi yake ni adhama na utukufu, na haki yake yadumu milele.
[4] Hufanya mambo makuu ambayo yatakumbukwa; Yahwe ni mwenye huruma na
neema. [5] Huwapa chakula wafuasi wake waaminifu. Siku zote atalikumbuka agano
lake. [6] Alionesha uweza wa kazi zake kwa watu wake kwa kuwapa urithi wa mataifa.
[7] Kazi za mikono yake ni za kuaminika na haki; maagizo yake yote ni ya kuaminika.
[8] Yamethibitika milele, yamefanywa katika uaminifu na vizuri. [9] Aliwapa ushindi
watu wake; aliliteuwa agano lake milele; jina lake ni takatifu na lakutisha. [10] Kumcha
Yahwe ni mwanzo wa hekima; wale washikao maagizo yake wana uelewa mzuri. Sifa
yake yadumu milele.

# 112

[1] Msifuni Yahwe. Amebarikiwa mtu yule anaye mtii Yahwe, apendezwaye sana
na amri zake. [2] Kizazi chake kitakuwa ni chenye nguvu duniani; kizazi cha mcha
Mungu kitabarikiwa. [3] Nyumbani mwake mna utajiri na mali; na haki yake itadumu
milele. [4] Nuru huangazia gizani kwa ajili ya mtu mcha Mungu; yeye ni wa fadhili,
huruma, na haki. [5] Heri atendaye fadhili na kukopesha, afanyaye mambo yake kwa
uaminifu. [6] Kwa maana hataondoshwa kamwe; mwenye haki atakumbukwa milele.
[7] Haogopi habari mbaya; ni jasiri, akimtumainia Yahwe. [8] Moyo wake ni mtulivu,
hana woga, mpaka aonapo ushindi dhidi ya watesi wake. [9] Huwapa masikini kwa

ukarimu; haki yake yadumu milele; atainuliwa kwa heshima. [10] Mtu mwovu ataona
haya na kukasirika; atasaga meno yake na kuyeyuka; tamaa ya wasio haki itapotea.

# 113

[1] Msifuni Yahwe. Msifuni yeye, enyi watumishi wa Yahwe; lisifuni jina la Yahwe.
[2] Litukuzwe jina la Yahwe, tangu sasa na hata milele. [3] Toka maawio ya jua hata
machweo yake, Jina la Yahwe lazima lisifiwe. [4] Yahwe ameinuliwa juu ya mataifa
yote, na utukufu wake wafika juu mbinguni. [5] Ni nani aliye kama Yahwe Mungu wetu,
aliye na kiti chake juu, [6] atazamaye chini angani na duniani? [7] Humwinua maskini
toka mavumbini na kumpandisha muhitaji kutoka jaani, [8] ili amketishe pamoja na
wakuu, pamoja na wakuu wa watu wake. [9] Humpa watoto wanamke aliye tasa,
humfanya yeye kuwa mama wa watoto mwenye furaha. Msifuni Yahwe!

# 114

[1] Israeli ilipotoka Misri, na nyumba ya Yakobo toka kutoka katika wale watu wa
kigeni, [2] Yuda ilifanyika kuwa mahali pake patakatifu, Ufalme wa Israeli. [3] Bahari
iliona ikakimbia; Yordani ilirudi nyuma. [4] Milima iliruka kama kondoo waume,
vilima viliruka kama wana-kondoo. [5] Ewe Bahari kwa nini ulikimbia? Yordani kwa
nini ulirudi nyuma? [6] Milima, kwa nini uliruka kama kondoo waume? Enyi vilima
wadogo, kwa nini mliruka kama wana-kondoo? [7] Tetemeka, ee nchi, mbele za Bwana,
uweponi mwa Mungu wa Yakobo. [8] Aligeuza mwamba kuwa ziwa la maji, jiwe gumu
kuwa chemchem.

# 115

[1] Sio kwetu, Yahwe, sio kwetu, bali kwa jina lako ulete heshima, kwa ajili ya
uaminifu wa agano lako na uaminifu wako. [2] Kwa nini mataifa yalazimike kusema,
“Yuko wapi Mungu wako?” [3] Mungu wetu aliye mbinguni; hufanya chochote
apendacho. [4] Sanamu za mataifa ni fedha na dhahabu, kazi ya mikono ya wanadamu.
[5] Sanamu hizo zina vinywa, lakini haziongei; zina macho, lakini hazioni; [6] zina
masikio, lakini hazisikii; zina pua lakini hazinusi. [7] Sanamu hizo zina mikono, lakini
hazishiki; zina miguu, lakini haziwezi kutembea; wala haziongei kutoka viywani
mwao. [8] Wale wanao zitengeneza wanafanana nazo, vile vile yeyote anaye amini
katika hizo. [9] Israeli, amini katika Yahwe; yeye ni msaada wako na ngao yako.
[10] Nyumba ya Haruni, amini katika Yahwe; yeye ni msaada wako na ngao yako.
[11] Ninyi mnao mheshumu Yahwe, mwamini yeye; yeye ni msaada wenu na ngao yenu.
[12] Yahwe hutukumbuka sisi na atatubariki; ataibariki familia ya Israeli; atabariki
familia ya Haruni. [13] Atawabariki wale wanao muheshimu yeye, wote vijana na
wazee. [14] Yahwe na awaongeze ninyi zaidi na zaidi, ninyi pamoja na watoto wenu.
[15] Yahwe na awabariki, aliyeziumba mbingu na nchi. [16] Mbingu ni za Yahwe; lakini
nchi amewapa wanadamu. [17] Wafu hawamsifu Yahwe, wala wote washukao chini
kwenye ukimya; [18] bali tutamtukuza Yahwe sasa na hata milele. Msifuni Yahwe.

# 116

[1] Nampenda Yahwe kwa kuwa anasikia sauti yangu na kuomba kwangu kwa ajili
ya huruma. [2] Kwa sababu alinisikiliza, nitamuita yeye ningali ninaishi. [3] Kamba
za mauti zilinizunguka, na mitego ya kuzimu ilinikabili; niliona dhiki na huzuni.
[4] Kisha niliita kwa jina la Yahwe: “Tafadhali Yahwe, uiokoe nafsi yangu.” [5] Yahwe
ni mwenye neema na haki; Mungu wetu ni mwenye huruma. [6] Yahwe huwalinda
wasio na hila; nilishushwa chini akaniokoa. [7] Nafsi yangu inaweza kurudi mahali
pake pa kupumzika, kwa kuwa Yahwe amekuwa mwema kwangu. [8] Kwa maana
uliokoa uhai wangu dhidi ya kifo, mcho yangu dhidi ya machozi, na miguu yangu

dhidi ya kujikwaa. [9] Nitamtumikia Yahwe katika nchi ya walio hai. [10] Nilimwamini
yeye, hata niliposema, "nimeteswa sana." [11] Kwa haraka nilisema, "Watu wote ni
waongo." [12] Nimlipeje Yahwe kwa wema wake wote kwangu? [13] Nitakiinua kikombe
cha wokovu, na kuliitia jina la Yahwe. [14] Nitatimiza viapo vyangu kwa Yahwe katika
uwepo wa watu wake wote. [15] Mauti ya wacha Mungu ina thamani machoni pa
Mungu. [16] Ee Yahwe, hakika, mimi ni mtumishi wako; mimi ni mtumishi wako,
mwana wa mjakazi wako; umefungua vifungo vyangu. [17] Nitakutolea dhabihu ya
shukrani na nitaliitia jina la Yahwe. [18] Nitatimiza viapo vyangu kwa Yahwe katika
uwepo wa watu wake wote, [19] katika nyua za nyumba ya Yahwe, katikati yako,
Yerusalemu. Msifuni Yahwe.

# 117

[1] Msifuni Yahwe, enyi mataifa yote; enyi watu mhimidini yeye. [2] Kwa kuwa
uaminifu wa agano lake ni mkuu kwetu, na uaminifu wa Yahwe wadumu milele.
Msifuni Yahwe.

# 118

[1] Mshukuruni Yahwe, kwa kuwa ni mwema, kwa maana uaminifu wa agano lake
wadumu milele. [2] Israeli na aseme, "Uaminifu wa agano lake wadumu milele."
[3] Nyumba ya Haruni na iseme, "Uaminifu wa agano lake wadumu milele." [4] Wafuasi
waaminifu wa Yahwe na waseme, "Uaminifu wa agano lake wadumu milele." [5] Katika
dhiki yangu nilimuita Yahwe; Yahwe alinijibu na kuniweka huru. [6] Yahwe yuko
pamoja nami; sitaogopa; mwanadamu atanifanya nini? Yahwe yuko upande wangu
kama msaidizi; [7] nitawatazama kwa ushindi wale walio nichukia. [8] Ni bora kuwa
na makazi katika Yahwe kuliko kumtumainia mwanadamu. [9] Ni bora kukimbilia
katika Yahwe kuliko kuamini katika wakuu. [10] Mataifa yote walinizunguka; kwa jina
la Yahwe niliwakatilia mbali. [11] Walinizunguka; naam, walinizunguka; kwa jina la
Yahwe niliwakatilia mbali. [12] Walinizunguka kama nyuki; walitoweka haraka kama
moto kati ya miiba; kwa jina la Yahwe niliwakatilia mbali. [13] Walinishambulia ili
waniangushe, lakini Yahwe alinisaidia. [14] Yahwe ni nguvu yangu na furaha yangu,
na ndiye anaye niokoa. [15] Kelele za ushindi zimesikika katika maskani ya wenye
haki; mkono wa kuume wa Mungu umeshinda. [16] Mkono wa kuume wa Mungu
umetukuka; mkono wa kuume wa Yahwe umeshinda. [17] Sitakufa, bali nitaishi na
kuyatangaza matendo ya Yahwe. [18] Yahwe ameniadhibu vikali; lakini hajaruhusu
nife. [19] Unifungulie milango ya haki; nitaingia na nitamshukuru Yahwe. [20] Hili
ni lango la Yahwe; wenye haki hupitia kwalo. [21] Nitakushukuru wewe, kwa kuwa
ulinijibu, na umekuwa wokovu wangu. [22] Jiwe ambalo wajenzi walilikataa wajenzi
limekuwa msingi. [23] Yahwe ndiye afanyaye hili; ni la ajabu machoni petu. [24] Hii
ni siku ambayo Yahwe ametenda; tutaifurahia na kuishangilia. [25] Tafadhali, Yahwe,
utupe ushindi! Tafadhali, Yahwe, utupe mafanikio! [26] Amebarikiwa yule ajaye katika
jina la Yahwe; tunakubariki kutoka katika nyumba ya Yahwe. [27] Yahwe ni Mungu, na
ametupa sisi nuru; ifungeni dhabihu kwa kamba pembeni mwa madhabahu. [28] Wewe
ni Mungu wangu, nami nitakushukuru; wewe ni Mungu wangu; nitakutukuza wewe.
[29] Oh, mshukuruni Yahwe; kwa kuwa ni mwema; kwa maana uaminifu wa agano
lake wadumu milele.

# 119

ALEPH. [1] Wamebarikiwa wale ambao njia zao hazina lawama, waenendao katika
sheria ya Yahwe. [2] Wamebarikiwa wale wazishikao amri zake thabiti, wamtafutao
kwa moyo wao wote. [3] Hawatendi makosa; wanaenenda katika njia zake. [4] Wewe
umetuamuru kuyashika maagizo yako ili tuyachunguze kwa umakini. [5] Oh,

ningependa njia zangu ziwe thabiti nizitii amri zako! 6 Ndipo sitaaibika nizifikiripo
amri zako zote. 7 Nitakushukuru wewe kwa unyofu wangu wa moyo nijifunzapo
amri za haki yako. 8 Nitazitii amri zako; usiniache peke yangu. BETH. 9 Ni jinsi
gani kijana aweza kuendelea kuishi katika njia yake ya utakatifu? Ni kwa kulitii
neno lako. 10 Kwa moyo wangu wote ninakutafuta wewe; Usiniache nipotee mbali
na maagizo yako. 11 Moyoni mwangu nimeliweka neno lako ili nisije nikakutenda
dhambi. 12 Umetukuka, Yahwe; unifundishe amri zako. 13 Kwa kinywa changu
nimetangaza amri ya haki yako yote ambayo umeifunua. 14 Ninafurahi katika njia
ya amri za agano lako zaidi kuliko katika utajiri. 15 Nitayatafakari maagizo yako
na kuzitilia maanani njia zako. 16 Ninafurahia katika amri zako; sitalisahau neno
lako. GIMEL. 17 Uwe mwema kwa mtumishi wako ili niweze kuishi na kulishika
neno lako. 18 Ufungue macho yangu ili niweze kuona mambo ya ajabu katika sheria
yako. 19 Mimi ni mgeni katika nchi; usizifiche amri zako mbali nami. 20 Moyo
wangu unauma kwa kutamani sana kuzijua amri zako za haki wakati wote. 21 Wewe
huwakemea wenye kiburi, waliolaaniwa, wanao tanga-tanga mbali na amri zako.
22 Uniokoe dhidi ya aibu na udhalilishaji, maana nimezitii amri za agano lako.
23 Ingawa watawala wanapanga njama na kunikashfu, mtumishi wako huzitafakali
amri zako. 24 Amri za agano lako ni furaha yangu, na washauri wangu. DALETH.
25 Uhai wangu unashikamana na mavumbi! nipe uhai kwa neno lako. 26 Nilikuambia
mapito yangu, na ulinijibu; nifundishe sheria zako. 27 Unifahamishe njia ya maagizo
yako, ili niweze kutafakari juu ya mafundisho yako ya ajabu. 28 Nimelemewa na
huzuni! Nitie nguvu kwa neno lako. 29 Uiondoe kwangu njia ya udanganyifu;
kwa wema wako unifundishe sheria yako. 30 Nimechagua njia ya uaminifu; siku
zote nimeweka amri za haki yako mbele yangu. 31 Ninashikamana na amri za
agano lako; Yahwe, usiniache niaibike. 32 Nitakimbia katika njia ya amri zako, kwa
sababu wausukuma moyo wangu kufanya hivyo. HE 33 Unifundishe, Yahwe, njia
za sheria yako, nami nitazishika hadi mwisho. 34 Unipe uelewa, nami nitazishika
sheria zako; nitazitii kwa moyo wangu wote. 35 Uniongoze katika njia ya amri
zako, maana ninafurahi kuenenda katika hizo. 36 Uelekeze moyo wangu kuzielekea
amari za agano lako na uniweke mbali na matendo yasiyo haki tena. 37 Uyageuze
macho yangu dhidi ya kutazama mambo yasiyofaa; unihuishe katika njia zako.
38 Umtendee mtumishi wako ahadi ambayo uliifanya kwa wale wanaokuheshimu
wewe. 39 Uniondolee shutumu niiogopayo, maana hukumu zako za haki ni njema.
40 Tazama, nimeyatamani maagizo yako; unihuishe katika haki yako. VAV. 41 Ee
Yahwe, unipe upendo wako usiokwisha na wokovu wako kulingana na ahadi yako;
42 ndipo nitakuwa na jibu kwa ajili ya yule anayenidhihaki. 43 Usiliondoe neno
la kweli mdomoni mwangu, maana nimesubiri kwa ajili ya amri zako za haki.
44 Nitazitii sheria zako siku zote, milele na milele. 45 Nitaenenda salama, maana
ninayatafuta maagizo yako. 46 Nitazinena amri zako thabiti mbele ya wafalme nami
sitaaibika. 47 Ninafurahia katika amri zako, nizipendazo sana. 48 Nitaziinulia mikono
yangu amri zako, nizipendazo; nitazitafakari sheria zako. ZAYIN. 49 Kumbuka ahadi
yako kwa mtumishi wako kwa sababu umenipa tumaini. 50 Hii ni faraja yangu
katika mateso: kuwa ahadi yako imeniweka hai. 51 Wenye kiburi wamenicheka,
lakini sijaiacha sheria yako. 52 Nimezitafakari amri zako za haki tangu zamani,
Yahwe, nami ninajifariji mwenyewe. 53 Hasira kali imenishikilia kwa sababu ya
waovu wanaoikataa sheria yako. 54 Sheria zako zimekuwa nyimbo zangu katika
nyumba ninayoishi kwa muda. 55 Ninalifikiria jina lako wakati wa usiku, Yahwe, na
kuzishika sheria zako. 56 Hili limekuwa zoezi langu kwa sababu nimeyatii maagizo
yako. HETH. 57 Yahwe ni sehemu yangu; nimeamua kuyatii maneno yake. 58 Kwa
bidii ninaomba neema yako kwa moyo wangu wote; unihurumie, kama neno lako

lilivyo ahidi. 59 Nilizichunguza njia zangu na kugeuzia miguu yangu kwenye amri
za agano lako. 60 Naharakisha na sichelewi kuzishika amri zako. 61 Kamba za
waovu zimenifunga; nami sijaisahau sheria yako. 62 Katikati ya usiku ninaamka
kukushukuru wewe kwa sababu ya amri za haki yako. 63 Ninaurafiki na wale wanao
kuabudu wewe, wale wote watiio maagizo yako. 64 Yahwe, nchi, imejaa uaminifu wa
agano lako; unifundishe sheria zako. TETH. 65 Wewe umemtendea mema mtumishi
wako, Yahwe, sawasawa na neno lako. 66 Unifundishe utambuzi sahihi na uelewa,
kwa kuwa nimeamini katika amri zako. 67 Kabla sijateswa nilipotea, lakini sasa
nimelitii neno lako. 68 Wewe ni mwema, na ndiye yule utendaye mema; unifundishe
sheria zako. 69 Wenye kiburi wamenichafua kwa uongo, lakini niliyashika maagizo
yako kwa moyo wangu wote. 70 Mioyo yao ni migumu, lakini ninafurahia katika
sheria yako. 71 Ni vizuri kwangu kuwa nimeteseka ili niweze kujifunza sheria zako.
72 Maagizo yatokayo kinywani mwako ni ya thamani zaidi kwangu kuliko maelfu ya
vipande vya dhahabu na fedha. YOD. 73 Mikono yako imeniumba na kunitengeneza;
unipe uelewa ili niweze kujifunza amri zako. 74 Wale wanao kucha wewe watafurahi
wanionapo kwa sababu ninapata tumaini katika neno lako. 75 Ninajua, Yahwe, kuwa
amri zako ni za haki, na kuwa katika uaminifu ulinitesa. 76 Agano lako aminifu
na linifariji, kama ulivyomwahidi mtumishi wako. 77 Unihurumie ili niweze kuishi,
kwa maana sheria yako ni furaha yangu. 78 Wenye kiburi na waaibishwe, maana
wamenitukana; bali mimi nitayatafakari maagizo yako. 79 Wale wote wanao kucha
wewe na wanigeukie, wale wazijuao amri za agano lako. 80 Moyo wangu uwe
mkamilifu pamoja na heshima kwa sheria zako ili nisiaibike. KAPH. 81 Ninazimia kwa
kutamani sana kuwa wewe unaweza kuniokoa! Ninamatumaini katika neno lako.
82 Macho yangu yanatamani sana kuiona ahadi yako; ni lini utanifariji mimi? 83 Kwa
maana nimekuwa kama kiriba katika moshi; sisahau sheria zako. 84 Ni kwa muda
gani gani mtumishi wako atalazimika kuyavumilia haya; ni lini utawahukumu wale
wanaonitesa? 85 Wenye kiburi wamenichimbia shimo, wasiotii sheria yako. 86 Amri
zako zote ni za kuaminika; wale watu walinitesa bila ya haki; unisaidie. 87 karibu
kunifanya nifikie mwisho juu ya nchi hii, lakini siyakatai maagizo yako. 88 Kwa
upendo wako thabiti, uniweke hai, ili niweze kuzitii amri zako. LAMEDH. 89 Yahwe,
neno lako linasimama milele; neno lako limefanywa imara mbinguni. 90 Uaminifu
wako wadumu kwa ajili ya vizazi vyote; umeiimarisha nchi, nayo inadumu. 91 Vitu
yote yaliendelea mpaka leo hii, kama vile ulivyosema katika amri zako za haki,
maana vitu vyote ni watumishi wako. 92 Kama sheria yako isingekuwa furaha yangu,
ningeangamia katika mateso yangu. 93 Sitayasahau kamwe maagizo yako, maana
kupitia hayo umeniweka hai. 94 Mimi ni wako, kwa maana ninayatafuta maagizo
yao. 95 Waovu hujiandaa kuniangamiza, lakini nitatafuta kuzielewa amri za agano
lako. 96 Nimeona kuwa kila kitu kina mipaka, lakini amri zako ni pana, zaidi ya
mipaka. MEM. 97 Oh ni jinsi gani naipenda sheria yako! Ni tafakari yangu mchana
kutwa. 98 Amri zako hunifanya mwenye hekima kuliko adui zangu, maana amri zako
siku zote ziko pamoja nami. 99 Ninauelewa zaidi kuliko walimu wangu wote, kwa
maana ninazitafakari amri za agano lako. 100 Ninaelewa kuliko wale wanaonizidi
umri; hii ni kwa sababu nimeyashika maagizo yako. 101 Nimeiepusha miguu yangu
na kila njia ya uovu ili niweze kulitii neno lako. 102 Sijaenda kinyume na amri zako
za haki, kwa maana wewe umenifundisha. 103 Ni jinsi gani maneno yako ni matamu
kwenye majaribu yangu, naam, matamu kuliko asali kinywani mwangu! 104 Kupitia
maagizo yako ninapata utambuzi; kwa hiyo kila njia isiyo ya kweli. 105 Neno lako ni
taa ya mguu miguu yangu na mwanga wa njia yangu. 106 Nimeapa na nimethibitisha,
kuwa nitazitii amri za haki yako. 107 Nimeteswa sana; uniweke hai, Yahwe, kama
ulivyoahidi katika neno lako. 108 Yahwe, tafadhali pokea dhabihu yangu ya hiari

ya kinywa changu, na unifundishe amri zako za haki. 109 Uhai wangu ziku zote
uko mkononi mwangu, lakini bado sisahau sheria yako. 110 Waovu wamenitegea
mtego, lakini sijapotea mbali na maagizo yako. 111 Nimezifanya amri za agano
lako kama urithi wangu milele, maana hizo ni furaha ya moyo wangu. 112 Moyo
wangu umewekwa kuzitii sheria zako milele mpaka mwisho kabisa. SAMEKH.
113 Ninawachukia watu wa kusita-sita, lakini naipenda sheria yako. 114 Wewe ni ficho
langu na ngao yangu; nalingoja neno lako. 115 Ondokeni kwangu, ninyi mtendao
uovu, ili niweze kuzitii amri za Mungu wangu. 116 Uniwezeshe kwa neno lako ili
niweze kuishi na nisiaibike na matumaini yangu. 117 Unisaidie, nami nitakuwa
salama; siki zote nitazitafakari sheria zako. 118 Wewe huwakataa wale wote wapoteao
mbali na sheria zako, maana watu hao ni wadanganyifu na si wakuaminika. 119 Wewe
huwaondoa waovu wa nchi kama takataka; kwa hiyo ninazipenda amri zako thabiti.
120 Mwili wangu hutetemeka kwa hofu yako, na ninaziogopa amri za haki yako. AYIN.
121 Ninafanya kilicho sahihi na haki; usiniache kwa watesi wangu. 122 Uwe mdhamini
wa ustawi wa mtumishi wako; usiwaache wenye kiburi wanionee. 123 Macho
yangu yanachoka kwa kuusubiri wokovu wako na neno lako la haki. 124 Mwoneshe
mtumishi wako uaminifu wa agano lako, na unifundishe sheria zako. 125 Mimi ni
mtumishi wako; unipe uelewa ili niweze kuzijua amri za agano lako. 126 Ni wakati wa
Yahwe kutenda, kwa maana watu wamevunja sheria yako. 127 Hakika ninazipenda
amri zako kuliko dhahabu, naam, kuliko dhahabu safi. 128 Hivyo ninayafuata maagizo
yako yote kwa makini, na ninachukia kila njia ya uongo. PE. 129 Sheria zako ni za
ajabu, ndiyo sababu ninazitii. 130 Ufafanuzi wa maneno yako huleta nuru; na kumpa
ufahamu mjinga. 131 Ninafungua kinywa changu na kutweta, maana ninazitamani
amri zako. 132 Unigeukie na unihurumie, kama ufanyavyo siku zote kwa wale
walipendao jina lako. 133 Uziongoze hatua zangu kwa neno lako; usiruhusu dhambi
yeyote initawale. 134 Unikomboe dhidi ya wanadamu waonevu ili niyatii maagizo
yako. 135 Uso wako umwangazie mtumishi wako, na unifundishe sheria zako. 136 Mito
ya machozi yatiririka kutoka machoni pangu kwa sababu watu hawaitii sheria yako.
TSADHE. 137 Wewe ni mwenye haki, Yahwe, na amri zako ni haki. 138 Umezipa
amri za agano lako haki na uaminifu. 139 Hasira imeniangamiza kwa sababu adui
zangu husahau maneno yako. 140 Neno lako limepimwa sana, naye mtumishi wako
analipenda. 141 Sina umuhimu na ninadharauliwa, lakini bado siyasahau maagizo
yako. 142 Hukumu yako ni ya haki milele, na sheria yako ni ya kuaminika. 143 Japo
dhiki na taabu vimenipata, amri zako bado ni furaha yangu. 144 Amri za agano
lako ni za haki milele; unipe uelewa ili niweze kuishi. QOPH. 145 Nililia kwa moyo
wangu wote, “Unijibu, Yahwe, nitazishika sheria zako. 146 Ninakuita wewe; uniokoe,
nami nitazitii amri za agano lako.” 147 NInaamka asubuhi kabla jua halijachomoza
na kulia kwa ajili ya msaada. 148 Ninatumaini katika maneno yako. Macho yangu
yako wazi usiku kucha ili niweze kutafakari juu ya neno lako. 149 Sikia sauti yangu
katika uaminifu wa agano lako; uniweke hai, Yahwe, kama ulivyoahidi katika amri
zako za haki. 150 Wale wanaonitesa wananikaribia, lakini wako mbali na sheria
yako. 151 Wewe uko karibu, Yahwe, na amri zako ni za kuaminika. 152 Muda mrefu
uliopita nilijifunza kutoka katika amri za agano lako ulizoziweka katika mahali pa
milele. RESH. 153 Uyatazame mateso yangu na unisaidie, maana siisahau sheria
yako. 154 Unitetee na kunikomboa; unihifadhi, kama ulivyo ahidi katika neno lako.
155 Wokovu uko mbali na waovu, maana hawazipendi amri zako. 156 Matendo yako
ya huruma ni makuu, Yahwe; uniweke hai; kama ufanyavyo siku zote. 157 Watesi
wangu na adui zangu ni wengi, lakini bado sijaenda mbali na amri za agano lako.
158 Nimewaona wasaliti wakitia kinyaa kwa sababu hawalishiki neno lako. 159 Tazama

jinsi niyapendavyo maagizo yako; uniweke hai, Yahwe, kama ulivyoahidi katika
uaminifu wa agano lako. 160 Kiini cha neno lako ni kweli; kila mmoja mwenye
amri za haki hudumu milele. SHIN. 161 Wakuu hunitesa bila sababu; moyo wangu
hutetemeka, ukiogopa kutolitii neno lako. 162 Ninalifurahia neno lako kama apataye
nyara nyingi. 163 Ninachukia na kudharau uongo, lakini naipenda sheria yako.
164 Mara saba kwa siku ninakusifu wewe kwa sababu ya amri zako za haki. 165 Wana
amani nyingi, waipendao sheria yako; hakuna cha kuwatia mashakani. 166 Naungoja
wokovu wako, Yahwe, na ninatii amri zako. 167 Ninazishika amri zako thabiti, na
ninazipenda sana. 168 Ninayashika maagizo yako na amri zako thabiti, kwa maana
unajua kila kitu nifanyacho. TAV. 169 Sikia kilio changu, Yahwe; unipe uelewa wa
neno lako. 170 Maombi yangu yaje mbele zako; unisaidie, kama ulivyoahidi katika
neno lako. 171 Midomo yangu na imwage sifa, maana wewe unanifundisha sheria
zako. 172 Ulimi wangu na uimbe kuhusu neno lako, maana amri zako zote ni za
haki. 173 Mkono wako unisaidie, maana nimechagua maagizo yako. 174 Ninautamani
wokovu wako, Yahwe, na sheria yako ni furaha yangu. 175 Naomba niishi na nikusifu
wewe, na amri zako za haki zinisaidie. 176 Nimetanga-tanga kama kondoo aliyepotea;
mtafute mtumishi wako, kwa maana sijazisahau amri zako.

# 120

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu. 1 Katika dhiki yangu nilimuita Yahwe, naye
akanijibu. 2 Uiokoe nasfi yangu, yahwe, dhidi ya wale wadanganyao kwa midomo yao
na wanenao hila kwa ndimi zao. 3 Yahwe atawaadhibu vipi, na atawafanyia kitu gani
zaidi, ninyi mlio na ulimi mdanganyifu? 4 Atawaadhibu kwa mishale ya shujaa iliyo
nolewa kwa makaa ya moto ya mretemu. 5 Ole wangu mimi kwa sababu ninaishi kwa
muda Mesheki; huko nyuma niliishi kati ya maskani ya Kedari. 6 Kwa muda mrefu
sana niliisha na wale waichukiao amani. 7 Nipo kwa ajili ya amani, lakini ninenapo,
wao wako kwa ajili ya vita.

# 121

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu. 1 Nitayainua macho yangu nitazame
milimani. Msaada wangu utatoka wapi? 2 Msaada wangu unatoka kwa Yahwe,
aliyezifanya mbingu na nchi. 3 Hatauacha mguu wako uteleze; yeye akulindaye
hatasinzia. 4 Tazama, mlinzi wa Israeli hatasinzia wala hatalala usingizi kamwe.
5 Yahwe ni mlinzi wako; Yahwe ni uvuli mkono wako wa kuume. 6 Jua halitakudhuru
wakati wa mchana, wala mwezi wakati wa usiku. 7 Yahwe atakulinda na madhara
yote, na ataulinda uhai wako. 8 Yahwe atakulinda katika yote ufanyayo sasa na hata
milele.

# 122

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu, wa Daudi. 1 Nilifurahi waliponiambia, “Na
twende kwenye Nyumba ya Yahwe.” 2 Ee Yerusalemu, miguu yetu imesimama ndani
ya malango yako! 3 Ee Yerusalemu, uliojengwa kama mji uliopangiliwa kwa umakini!
4 Makabila huenda juu Yerusalemu, makabila ya Yahwe; kama ushuhuda wa Israeli,
kulishukuru jina la Yahwe. 5 Huko viliwekwa viti vya hukumu, viti vya enzi vya
nyumba ya Daudi. 6 Ombeni kwa ajili ya amani ya Yerusalemu! “Wote wakupendao
wawe na amani. 7 Amani iwepo ndani ya kuta zako ili ikutetee, na wawe na amani
ndani ya ngome zako.” 8 Kwa ajili ya ndugu zangu na rafiki zangu nitasema, “Amani
iwe ndani yenu.” 9 Kwa ajili ya Yahwe Mungu wetu, nitatafuta mema kwa ajili yako.

## 123

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu. 1 Nakuinulia macho yangu, wewe uketiye
mbinguni. 2 Tazama, kama vile macho ya watumishi watazamapo kwenye mkono wa
Bwana wao, na kama macho ya mjakazi yatazamapo mkono wa bibi yake, ndivyo
hivyo macho yetu yanamtazama Yahwe mpaka atakapo tuhurumia. 3 Ee Yahwe,
utuhurumie, kwa maana tunadhalilishwa sana. 4 Tumeshibishwa mzaha wa wenye
kiburi na dharau ya wenye majivuno.

## 124

Wimbo wa kwenda kuabudu; wa Daudi. 1 "Kama Yahwe asingekuwa upande wetu,"
Israeli na aseme sasa, 2 "Kama asingekuwa Yahwe ambaye alikuwa upande wetu
wakati watu walipoinuka dhidi yetu, 3 basi wangekuwa wametumeza tungali hai
hasira yao lipozidi dhidi yetu. 4 Maji yangetugharikisha; mto ungetuzidia. 5 Kisha
maji yafurikayo yangetuzamisha." 6 Atukuzwe Yahwe, ambaye hajaruhusu tuwe
mawindo kwa meno yao. 7 Tumetoroka kama ndege mtegoni mwa wawindaji; mtego
umevunjika, nasi tumetoroka. 8 Msaada wetu uko katika Yahwe, aliyeziumba mbingu
na nchi.

## 125

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu. 1 Wale wamwaminio Yahwe ni kama mlima
Sayuni, hautikisiki, wadumu milele. 2 Kama milima inavyo izunguka Yerusalemu,
hivyo ndivyo Yahwe anavyo wazunguka watu wake sasa na hata milele. 3 Fimbo
ya uovu haitatawala katika nchi ya wenye haki. Vinginevyo wenye haki wanaweza
kukosea. 4 Ee Yahwe, utende wema kwa wale walio wema na wale walio wanyoofu
mioyoni mwao. 5 Lakini kwa wale wanaogeukia njia zao za upotovu, Yahwe
atawaondoa pamoja na watenda maovu. Amani iwe na Israeli.

## 126

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu. 1 Bwana alipowarejesha mateka wa Sayuni,
tulikuwa kama waotao ndoto. 2 Vinywa vyetu vilijawa na vicheko na ndimi zetu
zilijawa na kuimba. Kisha wakasema kati ya mataifa, "Yahwe amewatendea mambo
makuu." 3 Yahwe alitufanyia mambo makuu; ni furaha gani tuliyokuwa nayo! 4 Ee
Yahwe, uwarejeshe mateka wetu, kama vijito vya kusini. 5 Wale wapandao kwa
machozi watavuna kwa kelele za furaha. 6 Yeye aendaye akilia, akibeba mbegu kwa
ajili a kupanda, atarudi tena kwa kelele za furaha, akileta miganda yake.

## 127

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu, wa Solomoni. 1 Yahwe asipoijenga nyumba,
waijengao wafanya kazi bure. Yahwe asipoulinda mji, aulindaye afanya kazi bure.
2 Ni kazi bure kwa wewe unayeamka mapema, na kulala kwa kuchelewa, au kula
mkate kwa kuufanyia kazi ngumu, maana Yahwe huwapa chakula awapendao hata
wawapo usingizini. 3 Tazama, wana ni urithi kutoka kwa Yahwe, uzao wa tumbo ni
thawabu kutoka kwake. 4 Kama mishale mkononi mwa shujaa, ndivyo walivyo wana
wa ujanani. 5 Ni namna gani alivyo barikiwa mtu ambaye amelijaza podo lake hivyo.
Hata aibishwa pindi atakapo kabiliana na adui zake katika lango.

## 128

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu. 1 Amebarikiwa kila mtu amchaye Yahwe,
atembeaye katika njia zake. 2 Kazi ya mikono yako, wewe utaifurahia; utabarikiwa
na kufanikiwa. 3 Mke wako atakuwa kama mzabibu uzaao katika nyumba yako;
wanao watakuwa kama miche ya mimea ya mizeituni wakaapo kuzunguka meza

yako. 4 Ndiyo, hakika, mtu anaye muheshimu Yahwe atabarikiwa. 5 Mungu na
akubariki toka Sayuni; na uweze kuona mafanikio ya Yerusalemu siku zote za maisha
yako. 6 Uishi uwaone wana wa wanao. Amani iwe na Israli.

# 129

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu. 1 "Mara nyingi tangu ujana wangu
wamekuwa wakinishambulia," Israeli na iseme. 2 "Mara nyingi tangu ujana
wangu wamekuwa wakinishambulia, lakini hawajanishinda. 3 Wakulima wamekuwa
wakilima mgonngoni kwangu; wametengeneza matuta yao marefu. 4 Yahwe ni
mwenye haki; amezikata kamba za waovu." 5 Wote waaibishwe na kurudishwa
nyuma, wale wachukiao Sayuni. 6 Na wawe kama nyasi juu ya paa ambayo hunyauka
kabla hayajakua, 7 ambayo hayawezi kujaza mkono wa mvunaji wala kifua cha
mfunga miganda. 8 Wale wapitao karibu wasiseme, "Baraka za Mungu na ziwe juu
yako; Tunakubariki katika jina la Yahwe."

# 130

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu. 1 Toka ndani yangu ninakulilia, Yahwe.
2 Bwana, usikie sauti yangu; masikio yako na yasikie kwa makini kuomba kwangu
kwa ajili ya huruma. 3 Kama wewe, Yahwe, ungehesabu maovu, Bwana, ni nani
angesimama? 4 Lakini kwako kuna msamaha, ili uweze kuheshimiwa. 5 Ninamngoja
Yahwe, nafsi yangu inasubiri, na katika neno lake ninatumainia. 6 Nafsi yangu
inamngoja Bwana kuliko mlinzi aingojavyo asubuhi. 7 Israeli, umtumainie yahwe.
Yahwe ni wenye huruma, na yuko tayari kusamehe. 8 Ni yeye ambaye ataikomboa
istaeli dhidi ya dhambi zake zote.

# 131

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu; wa Daudi. 1 Yahwe, moyo wangu haujivuni
wala macho yangu hayana kuburi. Sina matarajio makubwa kwa ajili yangu
mwenyewe wala kujihofia kwa mambo ambayo yako juu ya uwezo wangu. 2 Hakika
nimejituliza na kuinyamazisha nafsi yangu; kama mtoto aliyeachishwa na mama
yake, nafsi yangu ndani yangu iko kama mtoto aliye achishwa. 3 Israeli, umtumainie
Yahwe sasa na hata milele.

# 132

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu. 1 Yahwe, kwa ajili ya Daudi kumbuka
mateso yake yote. 2 Kumbuka ndiye aliye mwapia Yahwe, aliweka nadhiri kwa
Shujaa wa Yakobo. 3 Alisema, sitaingia nyumbani mwangu wala sitaenda kitandani
mwangu, 4 sitayapa macho yangu usingizi wala kope zangu kupumzika 5 mpaka
nitakapopata mahali kwa ajili ya Yahwe, na maskani kwa ajili ya Shujaa wa Yakobo."
6 Tazama tulisikia kuhusu hilo katika Efrata; tuliipata katika konde la Yearimu.
7 Tutaingia katika maskani ya Mungu; tutasujudu miguuni pake. 8 Inuka, Ee Yahwe,
uje mahali pako pa kupumzika, wewe na sanduku la nguvu zako! 9 Makuhani wako
na wavikwe uadilifu; waaminifu wako washangilie. 10 Kwa ajili ya mtumishi wako
Daudi, usimuache mfalme wako uliye mpaka mafuta. 11 Yahwe alimwapia Daudi
kiapo cha uhakika, kiapo cha uhakika ambacho hatakivunja: "Nitamuweka mmoja
wa wazawa wako kwenye kiti chako cha enzi. 12 Kama wana wako watalishika agano
langu na sheria ambazo nitawafundisha, watoto wao pia watakaa kwenye kiti chako
cha enzi milele." 13 Hakika Yahwe ameichagua Sayuni, ameitamani kwa ajili ya
makao yake. 14 "Hapa ni mahali pangu pa kupumzika milele. Nitaishi hapa, kwa
kuwa ninapatamani. 15 Nitapabariki sana kwa mahitaji. Nitawatosheleza maskini

wake kwa mkate. [16] Nitawavisha makuhani wake kwa wokovu, waaminifu wake
watashangilia kwa furaha. [17] Hapo nitachipusha pembe kwa ajili ya Daudi na kuweka
taa juu kwa ajili ya mpakwa mafuta wangu. [18] Nitawavisha adui kwa aibu, bali juu
yake taji yake itang'aa."

# 133

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu, wa Daudi. [1] Tazama, jinsi ilivyo vema na
yakupendeza ndugu waishi pamoja, kwa umoja! [2] Ni kama mafuta mazuri kichwani
yashukayo ndevuni. Ndevu za Haruni, na yashukayo mpaka upindo wa mavazi yake.
[3] Ni kama umande wa Hermoni uangukao milimani pa Sayuni. Maana huko ndiko
Bwana alipoamuru baraka, naam uzima milele na milele.

# 134

Wimbo wa kwenda hekaluni kuabudu. [1] Njoni, mtukuzeni Yahwe, enyi nyote
watumishi wa Yahwe, ninyi mnaotumika hekaluni mwa Yahwe wakati wa usiku.
[2] Inueni mikono yenu patakatifu pake na mtukuzeni Yahwe. [3] Mungu na awabariki
toka Sayuni, yeye aliye ziumba mbingu na nchi.

# 135

[1] Msifuni Yahwe. Lisifuni jina la Yahwe. Msifuni yeye, enyi watumishi wa Yahwe,
[2] ninyi msimamao katika nyumba ya Yahwe, katika nyua za nyumba ya Mungu wetu.
[3] Msifuni Yahwe, kwa kuwa ni mwema; liimbieni sifa jina lake, maana ni vizuri
kufanya hivyo. [4] Kwa kuwa Yahwe amemchagua Yakobo kwa ajili yake mwenyewe,
Israeli kama urithi wake. [5] Najua ya kuwa Yahwe ni mkuu, na kwamba Bwana wetu
yuko juu ya miungu yote. [6] Chochote Yahwe apendacho, hufanya mbinguni, duniani,
katika bahari na katika vilindi vyote. [7] Hushusha mawingu kutoka mbali, akifanya
mianga ya radi kuongozana na mvua na kuleta upepo toka katika ghala yake. [8] Aliua
mzaliwa wa kwanza wa Misri, wote wanadamu na wanyama. [9] Alituma ishara na
maajabu kati yako Misri, dhidi ya Farao na watumishi wake wote. [10] Aliwashambulia
mataifa mengi na aliua wafalme wenye nguvu, [11] Sihoni mfalme wa Waamori na
Ogu mfalme wa Bashani na falme zote za Kanaani. [12] Alitupatia sisi nchi yao kama
urithi, urithi wa Israeli watu wake. [13] Jina lako, Yahwe, inadumu milele; Yahwe,
kumbukumbu lako vizazi hata vizazi. [14] Kwa kuwa Bwana huwatetea watu wake
na anahuruma juu ya watumishi wake. [15] Sanamu za mataifa ni fedha na dhahabu,
kazi ya mikono ya wanadamu. [16] Sanamu hizo zina vinywa, lakini haziongei; zina
macho, lakini hazioni; [17] zina masikio, lakini hazisikii, wala vinywani mwao hamna
pumzi. [18] Wale wazitengenezao wanafanana nazo, vilevile kila anaye zitumainia.
[19] Enyi kizazi cha Israeli, mtukuzeni Yahwe; kizazi cha Haruni, mtukuzeni Yahwe.
[20] Kizazi cha Lawi, mtukuzeni Yahwe. [21] Atukuzwe Yahwe katika Sayuni, yeye aishiye
Yerusalemu. Msifuni Yahwe.

# 136

[1] Oh, mshukuruni Yahwe; kwa kuwa ni mwema, kwa maana uaminifu wa agano
lake wadumu milele. [2] Oh, Mshukuruni Mungu wa miungu, kwa maana uaminifu wa
agano lake wadumu milele. [3] Oh, mshukuruni Bwana wa mabwana, kwa maana
uaminifu wa agano lake wadumu milele. [4] Mshukuruni yeye ambaye peke yake
hufanya maajabu makuu, kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu milele. [5] Yeye
aliyezifanya mbingu kwa hekima zake, kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu
milele. [6] Mshukuruni yeye alitetandaza nchi juu ya maji, kwa maana uaminifu wa
agano lake wadumu milele. [7] Yeye aliyefanya mianga mikubwa, kwa maana uaminifu
wa agano lake wadumu milele. [8] Mshukuruni yeye alipaye jua kutawala mchana, kwa

maana uaminifu wa agano lake wadumu milele. 9 Mwezi na nyota vitawale usiku,
kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu milele. 10 Mshukuruni yeye aliyewaua
wazaliwa wa kwanza wa Misri, kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu milele.
11 Akawatoa Waisraeli kati yao, kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu milele.
12 Kwa mkono hodari na mkono ulio nyooshwa, kwa maana uaminifu wa agano
lake wadumu milele. 13 Mshukuruni yeye aliyeigawa Bahari ya Shamu, kwa maana
uaminifu wa agano lake wadumu milele. 14 Na kuwapitisha Waisraeli katikati yake,
kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu milele. 15 Lakini akamtupa Farao na
jeshi lake katika Bahari ya Shamu, kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu
milele. 16 Mshukuruni yeye aliye waongoza watu wake jangwani, kwa maana
uaminifu wa agano lake ni wa milele. 17 Yeye aliyewaua wafalme wakuu, kwa maana
uaminifu wa agano lake ni wadumu milele. 18 Mshukuruni yeye aliyewaua wafalme
maarufu, kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu milele. 19 Sihoni mfalme wa
Waamori, kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu milele. 20 Na Ogu, mfalme wa
Bashani, kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu milele. 21 Mshukuruni yeye
aliyewapa nchi yao kama urithi, kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu milele.
22 Urithi wa Israel mtumishi wake, kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu
milele. 23 Yeye aliyetukumbuka na kutusaidia katika unyonge wetu, kwa maana
uaminifu wa agano lake wadumu milele. 24 Mshukuruni yeye ambaye ametupa
ushindi juu ya aui zetu, kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu milele. 25 Yeye
awapaye chakula viumbe hai wote, kwa maana uaminifu wa agano lake wadumu
milele. 26 Oh, mshukuruni Mungu wa mbinguni, kwa maana uaminifu wa agano lake
wadumu milele.

# 137

1 Kando ya mito ya Babeli tuliketi na tulilia tulipokumbuka kuhusu Sayuni.
2 Tulitundika vinubi vyetu kwenye miti ya Babylon. 3 Huko watekaji wetu walitaka
tuwaimbie, na wale walio tudhihaki walitutaka sisi tufurahi, wakisema, “Tuimbieni
moja ya nyimbo za Sayuni.” 4 Tungewezaje kuimba wimbo unaomuhusu Yahwe
katika nchi ya ugeni? 5 Kama nikikusahau wewe, Yerusalemu, basi mkono wangu
wa kuume na usahau ujuzi wake. 6 Ulimi wangu na ushikamane juu ya kinywa
changu kama nisipokufikiria tena, na kama sipendelei zaidi Yerusalemu kuliko
furaha yangu kuu. 7 Kumbuka, Ee Yahwe, kile walichofanya Waedomu siku ya
anguko la Yerusalemu. Walisema, “Ibomoeni, ibomoeni mpaka chini kwenye misingi
yake.” 8 Binti za Babeli, hivi karibuni wataharibiwa- mtu na abalikiwe, yeyote
atakaye walipizia yale mliotufanyia sisi. 9 Mtu na abarikiwe, yeyote achukuaye na
kusambaratisha watoto wenu juu ya jiwe.

# 138

Zaburi ya Daudi. 1 Nitakushukuru kwa moyo wangu wote; mbele ya miungu
nitakuimbia sifa. 2 Nitasujundu mbele ya hekalu lako takatifu na kulishukuru jina
lako kwa ajili ya uaminifu wa agano lako na kwa uaminifu wako. Umelifanya
muhimu zaidi neno lako na jina lako kuliko kitu chochote. 3 Siku ile niliyo kuita,
ulinijibu; ulinitia moyo na kuitia nguvu nafsi yangu. 4 Wafalme wote wa nchi
watakushukuru wewe, Yahwe, maana watasikia maneno kutoka kinywani mwako.
5 Hakika, wataimba kuhusu matendo ya Yahwe, kwa kuwa utukufu wa Yahwe ni
mkuu. 6 Maana ingawa Yahwe yuko juu, lakini anawajali wanyenyekevu, lakini
hawatambui wenye majivuno. 7 Nijapopita katikati ya hatari, wewe utauhifadhi uhai
wangu; utanyoosha mkono wako dhidi ya hasira ya adui zangu, na mkono wako wa

kuume utaniokoa. 8 Yahwe yuko pamoja nami hadi mwisho; uaminifu wa agano lako,
Yahwe, wadumu milele. Usiwaache wale ambao mikono yako imewaumba.

# 139

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya daudi. 1 Ee Yahwe, wewe umenichunguza,
na unanijua. 2 Wewe unajua nikaapo na niinukapo; unayajua mawazo yangu tokea
mbali sana. 3 Unachunguza wenendo wangu na kulala kwangu; unazijua njia zangu
zote. 4 Kabla hakujawa na neno kwenye ulimi wangu, wewe unalijua kabisa, Yahwe.
5 Nyuma yangu na mbele yangu unanizunguka na kuniwekea mkono wako. 6 Maarifa
hayo ni mengi yananizidi mimi; yako juu sana, nami siwezi kuyafikia. 7 Niende
wapi mbali na roho yako? Niende wapi niukimbie uwepo wako? 8 Kama nikipaa
mbinguni, uko huko; kama nikifanya kitanda changu Kuzimuni, tazama, uko huko.
9 Kama nikipaa kwa mbawa za asubuhi na kwenda kuishi pande za mwisho wa
bahari, 10 hata huko mkono wako utaniongoza, mkono wako wa kuume utanishika.
11 Kama nikisema, “Hakika giza litanifunika, na nuru inizungukayo itakuwa usiku,”
12 Hata giza lisingweza kuwa giza kwako. Usiku ungeng'aa kama mchana, maana giza
na nuru kwako vinafanana. 13 Wewe uliumba sehemu zangu za ndani; uliniumba
tumboni mwa mama yangu. 14 Nitakusifu, kwa maana nimeumbwa kwa jinsi ya
ajabu. Nafsi yangu yalijua hili vizuri sana. 15 Mifupa yangu haikusitirika kwako
nilipoumbwa kwa siri, nilipoumbwa kwa ustadi pande za chini za nchi. 16 Uliniona
ndani ya tumbo; siku zote zilizo pangwa kwangu ziliandikwa kitabuni mwako hata
kabla ya siku ya kwanza kutokea. 17 Ni jinsi gani mawazo yako ni ya thamani
kwangu, Mungu! Njinsi ilivyo kubwa jumla zake! 18 Kama nikijaribu kuyahesabu
ni mengi kuliko mchanga. Niamkapo bado niko na wewe. 19 Ee Mungu, kama
ungewaua waovu; ondokeni kwangu enyi watu wenye vurugu. 20 Wanakuasi wewe
na kutenda udanganyifu; adui zako wananena uongo. 21 Je, siwachukii hao, wale
wakuchukiao Yahwe? Je, siwadharau wale wanao inuka dhidi yako? 22 Nawachukia
kabisa; wamekuwa adui zangu. 23 Ee Mungu, unichunguze na kuujua moyo wangu;
unijaribu na uyajue mawazo yangu. 24 Uone kama kuna njia ya uovu ndani yangu,
na uniongoze katika njia ya milele.

# 140

Kwa kiongozi wa muziki. Zaburi ya Daudi. 1 Yahwe, uniokoe dhidi ya waovu;
unikinge dhidi ya watu wenye vurugu. 2 Wao wanapanga uovu mioyoni mwao;
wanasababisha mapigano kila siku. 3 Ndimi zao zinajeruhi kama nyoka; sumu
ya fira imo midomoni mwao. Selah 4 Ee Yahwe, unilinde dhidi ya mikono ya
waovu; unikinge na vurugu za watu wanaopanga kuniangusha. 5 Wenye majivuno
wameweka mtego kwa ajili yangu; wameeneza nyavu; wameweka kitanzi kwa ajili
yangu. Selah 6 Nilimwambia Yahwe, “Wewe ni Mungu wangu; usikie kilio changu
unihurumie.” 7 Ee Yahwe, Bwana wangu, wewe ni mwenye nguvu uwezaye kuniokoa;
hunifunika ngao kichwa changu siku ya vita. 8 Ee Yahwe, usiyatimize matakwa ya
waovu; usiruhusu njama zao kufanikiwa. Selah 9 Wale wanao nizunguka huinua
vichwa vyao; madhara ya midomo yao wenyewe na yawafunike. 10 Makaa ya
moto na yawaangukie; uwatupe motoni, kwenye shimo refu, wasiweze kuinuka
tena. 11 Watu wenye ndimi na wasifanywe salama juu ya nchi; na uovu umuwinde
kumpiga mtu mwenye vurugu mpaka afe. 12 Ninajua kuwa Yahwe atahukumu
kwa haki walioteswa, na kuwa atawapa haki wahitaji. 13 Hakika watu wenye haki
watalishukuru jina lako; watu wanyoofu wataishi uweponi mwako.

# 141

Zaburi ya Daudi. [1] Ee Yahwe, ninakulilia wewe; uje upesi kwangu. Unisikilize
nikuitapo. [2] Maombi yangu na yawe kama uvumba mbele zako; mikono yangu
iliyoinuliwa na iwe kama dhabihu ya jioni. [3] Ee Yahwe, uweke mlinzi kinywani
mwangu; mngojezi malangoni pa midomo yangu. [4] Usiruhusu tamaa ya moyo wangu
kutamani uovu wowote wala kushiriki katika matendo ya dhambi na watu waishio
maovuni. Nisile vyakula vyao vya anasa. [5] Mwenye haki na anipige; nao utakuwa
ni wema kwangu. Anirudi; itakuwa kama mafuta kichwani pangu; kichwa changu
na kisikatae kupokea. Lakini maombi yangu siku zote yatakuwa dhidi ya matendo
yao mauvu. [6] Viongozi wao watatupwa chini toka juu mlimani; watayasikia maneno
yangu kuwa ni matamu. [7] Watalazimika kusema, “Kama vile jembe moja livunjapo
ardhi, hivyo mifupa yetu imesambaratishwa kinywani pa kuzimu.” [8] Hakika macho
yangu yanakutazama wewe, Yahwe, Bwana; katika wewe napata kimbilio; usiiache
nafsi yangu. [9] Unilinde dhidi ya mitego waliyoiweka kwa ajili yangu, na matanzi yao
watendao maovu. [10] Waovu na waangukie kwenye nyavu zao wenywe pindi mimi
nitorokapo.

# 142

Zaburi ya Daudi, alipokuwa pangoni; maombi. [1] Kwa sauti yangu namlilia Yahwe
anisaidie; kwa sauti yangu naomba kwa ajili ya neema ya Yahwe. [2] Namwaga
malalamiko yangu mbele zake; ninamwambia shida zangu. [3] Roho yangu inapokuwa
dhaifu ndani yangu, wewe unajua mapito yangu. Kwenye njia niipitayo wamenifichia
mtego. [4] Natazama kulia kwangu na sioni yeyote anayenijali. Sina pa kukimbilia;
hakuna anayejali kuhusu uhai wangu. [5] Nilikuita wewe, Yahwe; nikasema, “Wewe
ni kimbilio langu, fungu langu katika nchi ya walio hai. [6] Sikia kuita kwangu, maana
nimeshushwa chini sana; uniokoe dhidi ya watesi wangu, maana wana nguvu kuliko
mimi. [7] Uitoe nafsi yangu kifungoni ili niweze kulishukuru jina lako. Wenye haki
watakusanyika karibu nami kwa sababu umekuwa mwema kwangu.”

# 143

Zaburi ya Daudi. [1] Ee Yahwe, usikie maombi yangu; sikia kuomba kwangu. Kwa
sababu ya uaminifu wa agano lako na haki yako, unijibu! [2] Usimuhukumu mtumishi
wako, kwa kuwa machoni pako hamna aliye haki. [3] Adui ameifuatia nafsi yangu;
amenisukuma hadi chini; amenifanya niishi gizani kama wale ambao wamekwisha
kufa siku nyingi zilizopita. [4] Na roho yangu inazidiwa ndani yangu; moyo wangu
unakata tamaa. [5] Nakumbuka siku za zamani zilizopita; nayatafakari matendo yako
yote; nawaza juu ya utimilifu wako. [6] Nakunyoshea mikono yangu katika maombi;
nafsi yangu inakuonea kiu katika nchi kavu. Selah [7] Unijibu upesi, Yahwe, kwa
sababu roho yangu inazimia. Usinifiche uso wako, vinginevyo nitakuwa kama wale
waendao chini shimoni. [8] Unifanye kusikia uaminifu wa agano lako wakati wa
asubuhi, maana ninakuamini wewe. Unionyeshe njia niipasayo kutembea kwayo,
kwa maana nakuinulia wewe nafsi yangu. [9] Uniokoe dhidi ya adui zangu, Yahwe;
nakimbilia kwako ili nijifiche. [10] Unifundishe kufanya mapenzi yako, maana wewe
ni Mungu wangu. Roho wako mwema na aniongoze mimi katika nchi ya unyoofu.
[11] Ee Yahwe, kwa ajili ya jina lako, unihifadhi hai; katika haki yako uitoe nafsi
yangu taabuni. [12] Katika uaminifu wa agano lako uwaondoshe maadui zangu na
uwaangamize maadui wa uhai wangu, maana mimi ni mtumishi wako.

# 144

Zaburi ya Daudi. [1] Atukuzwe Yahwe, mwamba wangu, anifundishaye mikono
yangu vita na vidole vyangu kupigana. [2] Wewe ni uaminifu wa agano langu na ngome
yangu, mnara wangu mrefu na uniokoaye, ngao yangu na yule ambaye katika yeye
napata kimbilio, uyatiishaye mataifa chini yangu. [3] Ee Yahwe, mtu ni kitu gani hata
umtazame au mwana wa mtu hata umfikirie? [4] Mtu ni kama pumzi, siku zake ni kama
uvuli upitao. [5] Ee Yahwe uziinamishe mbingu na ushuke chini, uiguse milima na
uifanye kutoa moshi. [6] Utume umeme uwatawanye adui zangu; upige mishale yako
na uwavuruge. [7] Nyosha mkono wako toka juu; uniokoe kutoka katika maji mengi,
na kutoka katika mkono wa wageni. [8] vinywa vyao hunena uongo, na mkono wao
wa kuume ni mkono wa uongo. [9] Nitakuimbia wimbo mpya, Mungu; kwa kinanda
cha nyuzi kumi nitakuimbia sifa wewe, [10] uwapaye wafalme wokovu, uliye muokoa
Daudi mtumishi wako dhidi ya upanga wa uovu. [11] Uniokoe na unitoe mkononi mwa
wageni. Midomo yao huongea uongo, na mkono wao wa kuume ni mkono wa uongo.
[12] Wana wetu na wawe kama mimea ikuayo kwa ukumbwa timilifu katika ujana
wao na binti zetu kama nguzo za pembeni, zilizonakishiwa kwa kupamba jumba
la kifahari. [13] Ghala zetu na zijae akiba ya kila aina ya mazao, na kondoo wetu
wazae elfu na makumi elfu mashambani mwetu. [14] Kisha ng'ombe wetu watakuwa
na nddama wengi. Hakuna atakayevunja kuta zetu; hakutakuwa na uhamisho wala
kilio mitaani mwetu. [15] Wamebarikiwa watu wenye baraka hizo; furaha ina watu
ambao Mungu wao ni Yahwe.

# 145

Zaburi ya sifa. Ya Daudi. [1] Nitakutukuza wewe, Mungu wangu, Mfalme;
nitalihimidi jina lako milele na milele. [2] Kila siku nitakuhimidi; nitalisifu jina
lako milele na milele. [3] Yahwe ndiye mkuu na wakusifiwa sana; ukuu wake
hauchunguziki. [4] Kizazi kimoja kitayasifu matendo yako kwa kizazi kijacho na
kitatangaza matendo yako makuu. [5] Nitaitafakari fahari ya utukufu wa adhama
yako na matendo yako ajabu. [6] Watanena juu ya nguvu ya kazi zako za kutisha,
nami nitatangaza ukuu wako. [7] Nao watatangaza wingi wa wema wako, na wataimba
kuhusu haki yako. [8] Yahwe ni wa neema na huruma, si mwepesi wa hasira na mwingi
katika uaminifu wa agano lake. [9] Yahwe ni mwema kwa wote; huruma zake zi juu ya
kazi zake zote. [10] Vyote ulivyo viumba vitakushukuru wewe, Yahwe; waaminifu wako
watakutukuza wewe. [11] Waaminifu wako watanena juu ya utukufu wa ufalme wako,
na watahubiri juu ya nguvu zako. [12] Watayafanya matendo makuu ya Mungu ya
julikane na wanadamu na utukufu wa fahari ya ufalme wake. [13] Ufalme wako ni wa
milele, na mamlaka yako ya dumu kizazi hata kizazi. [14] Yahwe huwategemeza wote
waangukao na huwainua wote walioinama chini. [15] Macho ya wote yanakungoja
wewe; nawe huwapa chakula chao kwa wakati sahihi. [16] Huufungua mkono wako
na hukidhi haja ya kila kiumbe hai. [17] Yahwe ni mwenye haki katika njia zake zote na
neema katika yote afanyayo. [18] Yahwe yu karibu na wote wamwitao, wale wamwitao
yeye katika uaminifu. [19] Hutimiza haja za wale wanao mheshimu yeye; husikia kilio
chao na kuwaokoa. [20] Yahwe huwalinda wale wampendao, lakini atawaangamiza
waovu wote. [21] Kinywa changu kitazinena sifa za Yahwe; wanadamu wote na
walitukuze jina lake takatifu milele na milele.

# 146

[1] Msifu Yahwe. Msifu Yahwe, ee nafsi yangu. [2] Ninamsifu Mungu maisha yangu
yote; nitamuimbia sifa Mungu wangu ni ngali ni hai. [3] Msiweke imani katika wakuu
au wanadamu, ambaye katika yeye hamna wokovu. [4] Wakati uhai wa pumzi ya mtu

unapokoma, hurudi aridhini; siku hiyo mipango yake hufikia mwisho. [5] Amebarikiwa
yule ambaye Mungu wa Yakobo ni msaada wake, ambaye tumaini lake liko katika
Yahwe Mungu wake. [6] Yahwe aliumba mbingu na nchi, bahari, na vyote vilivyomo;
huitazama kweli milele. [7] Yeye hutekeleza hukumu kwa ajili ya walioonewa na
huwapa chakula wenye njaa. Yahwe huwafungua waliofungwa; [8] Yahwe huyafungua
macho ya kipofu; Yahwe huwainua walioinama; Yahwe huwapenda watu wenye haki.
[9] Yahwe huwalinda wageni katika nchi; huwainua yatima na wajane, bali huipinga
njia ya wasio haki. [10] Yahwe atatawala milele, Mungu wako, Sayuni, kwa vizazi vyote.
Msifuni Yahwe.

# 147

[1] Msifuni Yahwe, kwa maana ni vyema kumwimbia sifa Mungu wetu, ni kuzuri,
kusifu kwa faa sana. [2] Yahwe huijenga tena Yerusalemu, huwakusanya pamoja watu
wa Israeli waliotawanyika. [3] Huponya mioyo iliyopondeka na kuganga majeraha
yao. [4] Huzihesabu nyota, naye huzipa majina zote. [5] Ukuu ni wa Bwana wetu na
nguvu zake ni za kutisha, ufahamu wake hauwezi kupimika. [6] Yahwe huwainua
wanyonge, huwashusha chini wenye jeuri. [7] Mwimbieni Yahwe kwa shukurani,
mwimbieni sifa Mungu wetu kwa kinubi. [8] Huzifunika mbingu kwa mawingu na
huiandaa mvua kwa ajili ya nchi, akizifanya nyasi kukua juu ya milima. [9] Huwapa
wanyama chakula na wana kunguru waliapo. [10] Hapati furaha katika nguvu ya farasi,
wala haridhii miguu imara ya mwanadamu. [11] Yahwe huridhia katika wale wanao
muheshimu yeye, watumainio katika uaminifu wa agano lake. [12] Msifuni Yahwe,
Yerusalemu, msifuni Mungu wenu, Sayuni. [13] Maana yeye huyakaza mapingo ya
malango yako, huwabariki watoto wako kati yako. [14] Huletamafanikio ndani ya
mipaka yako, hukutosheleza kwa ngano bora. [15] Huipeleka amri yake juu ya nchi,
amri zake hupiga mbio sana. [16] Huifanya theluji kama sufu, huitawanya barafu
kama majivu. [17] Hutupa mvua ya mawe kama makombo, ni nani awezaye kuhimili
baridi aitumayo? [18] Hutuma amri zake na kuziyeyusha, huvumisha upepo wake na
hutiririsha maji. [19] Hutangaza neno lake kwa Yakobo, amri zake na hukumu zake
kwa Israeli. [20] Hajafanya hivyo kwa taifa linginelo lolote, na kama ilivyo amri zake,
hawazijui. Msifuni Yahwe.

# 148

[1] Msifuni Yahwe. Msifuni Yahwe, ninyi mlio katika mbingu; msifuni yeye, ninyi
mlio juu. [2] Msifuni yeye, enyi malaika wake wote; msifuni yeye, majeshi ya malaika
wake wote. [3] Msifuni yeye, enyi jua na mwezi; msifuni yeye, nyota zote zing'aazo.
[4] Msifuni yeye, enyi mbingu zilizo juu zaidi na maji yaliyo juu ya anga. [5] Na vilisifu
jina la Yahwe, maana aliamuru, navyo vikaumbwa. [6] Pia ameviimrisha milele na
milele; naye alitoa amri ambayo haitabadilika. [7] Msifuni yeye kutoka nchi, ninyi
viumbe wa baharini na viumbe vyote katika kina cha bahari, [8] moto na mvua
ya mawe, theluji na mawingu, upepo wa dhoruba ukitimiza neno lake. [9] Msifuni
yeye, enyi milima na vilima, miti ya matunda na mierezi yote, [10] wanyama pori na
wanyama wafugwao, viumbe vitambaavyo na ndege. [11] Msifuni Yahwe, wafalme wa
nchi na mataifa yote, wakuu na watawala wote wa nchi, [12] wote vijana wa kiume na
vijana wa kike, wazee na watoto. [13] Na walisifu jina la Yahwe, kwa kuwa jina lake
pekee limetukuka na utukufu wake umeongezwa juu ya nchi na mbingu. [14] Naye
ameyainua mapembe ya watu wake kwa ajili ya sifa kutoka kwa waaminifu wake
wote, Waisraeli, watu wa karibu naye. Msifuni Yahwe.

## 149

[1] Msifuni Yahwe. Mwimbieni Yahwe wimbo mpya; imbeni sifa zake katika
kusanyiko la waaminifu. [2] Israeli ishangilie katika yeye aliye iumba; watu wa
Sayuni na washangilie katika mfalme wao. [3] Nao walisifu jina lake kwa kucheza;
na wamuimbie sifa yeye kwa ngoma na kinubi. [4] Kwa kuwa Yahwe hupata furaha
katika watu wake; huwapa utukufu wanyeyekevu kwa wokovu. [5] Wacha Mungu
wauchangilie ushindi; nao waimbe kwa furaha vitandani mwao. [6] Sifa za Mungu na
ziwe vinywani mwao na panga mbili zenye makali mkononi mwao [7] kutekeleza kisasi
juu ya mataifa na matendo ya adhabu juu ya watu. [8] Nao watawafunga wafalme wao
kwa minyororo na wakuu wao kwa pingu za chuma. Watatekeleza hukumu ambayo
imeandikwa. [9] Hii itakuwa ni heshima kwa ajili ya watakatifu wake wote. Msifuni
Yahwe.

## 150

[1] Msifuni Yahwe. Msifuni Yahwe katika patakatifu pake; msifuni katika mbingu za
ukuu wake. [2] Msifuni yeye kwa matendo yake makuu; msifuni yeye kwa kadri ya
wingi wa ukuu wake. [3] Msifuni kwa mlipuko wa pembe; msifuni kwa kinanda na
kinubi. [4] Msifuni kwa ngoma na kucheza; msifuni kwa vyombo vya nyuzi na filimbi.
[5] Msifuni kwa matoazi yavumayo; msifuni kwa matoazi avumayo sana. [6] Kila kilicho
na pumzi kimsifu Yahwe. Msifuni Yahwe.

# Mithali

1 Mithali za Sulemani mwana wa Daudi, mfalme wa Israeli. 2 Mithali hizi
zinafundisha hekima na maarifa, kufundisha maneno ya busara, 3 ili mpate maarifa
kwa ajili ya kuishi kwa kutenda wema, haki na adili. 4 Mithali hizi zinatoa hekima
kwa wale ambao hawakufunzwa, na kuwapa vijana maarifa na hadhari. 5 Watu
wenye busara wasikie na kuongeza elimu yao na watu wenye ufahamu wapate
mwongozo, 6 kwa kuelewa mithali, misemo, vitendawili na maneno ya wenye busara.
7 Hofu ya Yehova ni chanzo cha maarifa- wapumbavu hudharau hekima na nidhamu.
8 Mwanangu, sikia fundisho la baba yako na wala usiziache kanuni za mama yako;
9 zitakuwa kilemba cha neema katika kichwa chako na jebu zinazoning'inia kwenye
shingo yako. 10 Mwanangu wenye dhambi wakikushawishi katika dhambi zao, kataa
kuwafuata. 11 Kama watasema, “ haya tufuatae, tuvizie ili kufanya mauaji, tujifiche
ili tuwashambulie watu wasio na hatia, pasipo sababu. 12 Haya tuwameza wakiwa
hai, kama kuzimu inavyowachukua wenye afya, na kuwa kama wale waangukao
kwenye shimoni. 13 Tutapata vitu vyote vya thamani; tutazijaza nyumba zetu vile
tunavyoiba kwa wengine. 14 Weka vitu vyako kwetu; tutakuwa na mfuko moja kwa
pamoja.” 15 Mwanangu, usitembee katika njia moja pamoja nao; usiruhusu mguu
wako kugusa katika mapito yao; 16 miguu ya hukimbilia mabaya na huharakisha
kumwaga damu. 17 Kwa kuwa haina maana kumtegea ndege mtego wakati ndege
anaona. 18 Watu hawa huvizia kujiua wenyewe—wanatega mtego kwa ajili yao
wenyewe. 19 Ndivyo zilivyo njia za kila ambaye hupata utajiri kwa udhalimu; mapato
ya udhalimu huondoa uhai wa wenye utajiri. 20 Hekima inalia kwa sauti mtaani,
inapaza sauti katika viwanja; 21 katika mitaa inalia kwa sauti kuu, kwenye maingilio
ya milango ya mji inasema “ 22 Mpaka lini enyi wajinga mtapenda kuwa wajinga?
Mpaka lini enyi wenye dhihaka mtapenda dhihaka, na hadi lini enyi wapumbavu,
mtachukia maarifa? 23 Zingatia karipio langu; nitatoa mawazo yangu kwa ajili
yenu; nitawafahamisha maneno yangu. 24 Nimeita, nanyi mkakataa kusikiliza;
nimeunyosha mkono wangu, wala hakuna aliyezingatia. 25 Lakini mumedharau
mafundisho yangu yote na wala hamkuzingatia maelekezo yangu. 26 Nitacheka katika
taabu yenu, nitawadhihaki wakati wa kupatwa taabu- 27 hofu ya kutisha itawapata
kama tufani na maafa yatawakumba kama upepo wa kisulisuli, taabu na uchungu
vitawapata. 28 Halafu wataniita, nami sitawajibu; wataniita katika hali ya kukata
tamaa lakini hawataniona. 29 Kwa sababu wamechukia maarifa na hawakuchagua
kuwa na hofu ya Yehova, 30 hawakufuata mafundisho yangu na wakayadharau
masahihisho yangu yote. 31 Watakula matunda ya njia zao, na watashibishwa kwa
matunda ya hila zao wenyewe. 32 kwa maana wajinga hufa wanaporudi nyuma,
na kutojali kwa wapumbavu kutawaangamiza. 33 Bali kila anisikilizaye ataishi kwa
usalama na atapumzika salama pasipo hofu ya maafa.

## 2

1 Mwanangu, kama ukiyapokea maneno yangu na kuzitunza amri zangu, 2 usikilize
hekima na utaelekeza moyo wako katika ufahamu. 3 kama utalilia ufahamu na
kupaza sauti yako kwa ajili ya ufahamu, 4 kama utautafuta kama fedha na kupekua
ufahamu kama unatafuta hazina iliyojificha, 5 ndipo utakapofahamu hofu ya Yehova
na utapata maarifa ya Mungu. 6 Kwa kuwa Yohova hutoa hekima, katika kinywa
chake hutoka maarifa na ufahamu. 7 Yeye huhifadhi sauti ya hekima kwa wale
wampendezao, yeye ni ngao kwa wale waendao katika uadilifu, 8 huongoza katika

njia za haki na atalinda njia ya waaminifu kwake. 9 Ndipo utakapoelewa wema,
haki, usawa na kila njia njema. 10 Maana hekima itaingia moyoni mwako na maarifa
yataipendeza nafsi yako. 11 Busara itakulinda, ufahamu utakuongoza. 12 Vitakuokoa
kutoka katika njia ya uovu, kutoka kwa wale waongeao mambo potovu. 13 Ambao
huziacha njia za wema na kutembea katika njia za giza. 14 Hufurahia wanapotenda
maovu na hupendezwa katika upotovu. 15 Hufuata njia za udanganyifu na kwa
kutumia ghilba huficha mapito yao. 16 Busara na hekima zitakuokoa kutoka kwa
mwanamke malaya, kutoka kwa mwanamke anayetafuta visa na mwenye maneno
ya kubembeleza. 17 Yeye humwacha mwenzi wa ujana wake na kusahau agano la
Mungu wake. 18 Maana nyumba yake huinama na kufa na mapito yake yatakupeleka
kwa wale walioko kaburini. 19 Wote waiendeao njia yake hawatarudi tena na wala
hawataziona njia za uzima. 20 kwa hiyo utatembea katika njia ya watu wema na
kufuata njia za wale watendao mema. 21 Kwa wale watendao mema watafanya
makazi yao katika nchi, na wale wenye uadilifu watadumu katika nchi. 22 Lakini
waovu wataondolewa katika nchi na wale wasioamini wataondolewa katika nchi.

# 3

1 Mwanangu, usizisahau amri zangu na uyatunze mafundisho yangu katika moyo
wako, 2 maana ziatakuongezea siku zako na miaka ya maisha yako na amani.
3 Usiache utiifu wa agano na uaminifu viondoke kwako, vifunge katika shingo
yako, viandike katika vibao vya moyo wako. 4 Ndipo utapata kibali na heshima
mbele Mungu na wanadamu. 5 Mtegemee Yehova kwa moyo wako wote na wala
usitegemee ufahamu wako mwenyewe, 6 katika njia zako zote mkiri Yeye na yeye
atayanyosha mapito yako. 7 Usiwe mwenye busara machoni pako mwenyewe;
mche Yehova na jiepushe na uovu. 8 Itakuponya mwili wako na kukuburudisha
mwili wako. 9 Mheshimu Yehova kwa utajiri wako na kwa malimbuko ya mazao
kwa kila unachozalisha, 10 na ndipo ghala zako zitajaa na mapipa makubwa
yatafurika kwa divai mpya. 11 Mwanangu, usidharau kuadibishwa na Yohova na wala
usichukie karipio lake, 12 maana Yehova huwaadibisha wale wapendao, kama baba
anavyoshughulika kwa mtoto wake ampendezaye. 13 Yeye apataye hekima anafuraha,
naye hupata ufahamu. 14 Kwani katika hekima unapata manufaa kuliko ukibadilisha
kwa fedha na faida yake inafaa zaidi kuliko dhahabu. 15 Hekima inathamani zaidi
kuliko kito, na hakuna unachokitamani kinaweza kulinganishwa na hekima. 16 Yeye
anasiku nyingi katika mkono wake wa kuume; na mkono wake wa kushoto ni utajiri
na heshima. 17 Njia zake ni njia za ukarimu na mapito yake ni amani. 18 Yeye ni
mti wa uzima kwa wale wanaomshikilia, wale wanaomshikilia wanafuraha. 19 Kwa
hekima Yehova aliweka msingi wa dunia, kwa ufahamu aliziimarisha mbingu. 20 Kwa
maarifa yake vina vilipasuka na mawingu kudondosha umande wake. 21 Mwanangu,
zingatia hukumu ya kweli na ufahamu, na wala usiache kuvitazama. 22 Vitakuwa
uzima wa nafsi yako na urembo wa hisani wa kuvaa shingoni mwako. 23 Ndipo
utatembea katika njia yako kwa usalama na mguu wako hautajikwaa; 24 ulalapo
hutaogopa; utakapolala, usingizi wako utakuwa mtamu. 25 Usitishwe na hofu ya
ghafula au uharibifu uliosababishwa na waovu unapotokea, 26 kwa maana Yehova
utakuwa upande wako na ataulinda mguu wako usinaswe kwenye mtego. 27 Usizuie
mema kwa wale wanaoyastahili, wakati utendaji upo ndani ya mamlaka yako.
28 Jirani yako usimwambie, “Nenda, na uje tena, na kesho nitakupa,” wakati pesa
unazo. 29 Usiweke mpango wa kumdhuru jirani yako- anayeishi jirani nawe na
yeye anakuamini. 30 Usishindane na mtu pasipo sababu, ikiwa hajafanya chochote
kukudhuru. 31 Usimhusudu mtu jeuri au kuchagua njia zake zozote. 32 Maana mtu
mjanja ni chukizo kwa Yehova, bali humleta mtu mwaminifu kwenye tumaini lake.

33 Laana ya Yehova ipo katika nyumba ya watu waovu, bali huibariki maskani ya
watu wenye haki. 34 Yeye huwadhihaki wenye dhihaka, bali huwapa hisani watu
wanyenyekevu. 35 Watu wenye busara huirithi heshima, bali wapumbavu huinuliwa
kwa fedheha yao wenyewe.

# 4

1 Wanangu, sikilizeni, fundisho la baba, na zingatieni ili mjue maana ya ufahamu.
2 Mimi ninawapa mafundisho mazuri; msiyaache mafundisho yangu. 3 Mimi
nilikuwa mwana kwa baba yangu, mpole na mtoto pekee kwa mama yangu, 4 baba
alinifundisha akiniambia, “Moyo wako uzingatie sana maneno yangu; shika amri
zangu nawe uishi. 5 Jipatie hekima na ufahamu; usisahau na kuyakataa maneno
ya kinywa changu; 6 usiiache hekima nayo itakulinda; ipenda nayo itakuhifadhi
salama. 7 Hekima ni kitu cha muhimu sana, hivyo jipatie hekima na tumia namna
zote kuweza kupata ufahamu. 8 Tunza hekima nayo itakutukuza; ikumbatie nayo
itakuheshimu. 9 Hekima itaweka kilemba cha heshima juu ya kichwa chako; itakupa
taji zuri. 10 Mwanangu, sikiliza, na kuzingatia maneno yangu, nawe utapata miaka
mingi ya maisha yako. 11 Ninakuelekeza katika njia ya hekima, nimekuongoza katika
mapito yaliyonyooka. 12 Unapotembea, hakuna atakayesimama katika njia yako na
kama ukikimbia hutajikwaa. 13 Shika mwongozo wala usiuache, utakuongoza, maana
ni uzima wako. 14 Usifuate njia ya waovu wala usiende katika njia ya watendao uovu.
15 Jiepushe nayo, usipite katika njia hiyo; geuka na upite njia nyingine. 16 Maana
hawawezi kulala mpaka wafanye ubaya na hupotewa na usingizi hadi wasababishe
mtu kujikwaa. 17 Maana wao hula mkate wa uovu na hunywa divai ya vurugu. 18 Bali
njia ya mwenye kutenda haki ni kama mwanga ung'aao, huangaza zaidi na zaidi
hadi mchana inapowasili kwa ukamilifu. 19 Njia ya waovu ni kama giza - hawajui
ni kitu gani huwa wanajikwaa juu yake. 20 Mwanangu, zingatia maneno yangu;
sikiliza kauli zangu. 21 Usiziache zikaondoka machoni pako; uzitunze katika moyo
wako. 22 Maana maneno yangu ni uzima kwa wenye kuyapata na afya katika mwili
wao. 23 Ulinde salama moyo wako na uukinge kwa bidii zote; kwa kuwa katika moyo
hububujika chemichemi za uzima. 24 Jiepushe na kauli za udanganyifu na ujiepushe
na mazungumzo ya ufisadi. 25 Macho yako yatazame mbele kwa unyoofu na kwa
uthabiti tazama mbele sawasawa. 26 Usawazishe pito la mguu wako; na njia zako
zote zitakuwa salama. 27 Usigeuke upande wa kulia au kushoto; ondoa mguu wako
mbali na uovu.

# 5

1 Mwanangu, zingatia hekima yangu; sikiliza kwa makini ufahamu wangu, 2 ili
ujifunze busara na midomo yako iweze kuhifadhi maarifa. 3 Maana midomo ya
malaya hutiririsha asali na kinywa chake ni laini kuliko mafuta, 4 lakini mwishoni
anakuwa mchungu kama mnyoo, hukata kama upunga mkali. 5 Miguu yake huelekea
mauti; hatua zake huelekea njia yote ya kuzimu. 6 Hafikirii njia ya uzima. Hatua za
miguu yake hupotea, maana hajui anakwenda wapi. 7 Sasa, wanangu, nisikilizeni;
wala msiache kusikiliza maneno ya kinywa changu. 8 Lindeni njia yenu mbali naye
wala msiende karibu na mlango wa nyumba yake. 9 Kwa njia hiyo hamtawapa
wengine heshima yenu au miaka ya uzima wenu kwa mtu mkatiri; 10 wageni
usije kufanya karamu kwa utajiri wenu; kazi mliyoifanya haitaenda katika nyumba
ya wageni. 11 Mwishoni mwa maisha yenu mtajuta ambapo nyama na mwili
wenu vitaangamia. 12 Nanyi mtasema, “ Namna gani nilichukia fundisho na moyo
wangu ulidharau sahihisho! 13 Sikuweza kuwatii walimu wangu au kuwasikiliza
walionielekeza. 14 Nilikuwa nimeharibika kabisa katikati ya kusanyiko, miongoni

mwa makutano ya watu.” 15 Munywe maji kutoka kwenye birika lenu mwenyewe na
munywe maji yanatiririka kutoka kwenye kisima chenu. 16 Je inapaswa chemichemi
yenu ifurike popote na mifereji yenu ya maji itiririke katika njia kuu? 17 Yawe
yenu wenyewe peke yenu wala si kwa wageni. 18 Chemichemi yako ibarikiwe na
umfurahie mke wa ujana wako. 19 Maana ni ayala apendezaye na kulungu mwenye
uzuri. Matiti yake na yakujaze furaha muda wote; daima na utekwe na upendo
wake. 20 Mwanangu, kwa nini uwe mateka wa malaya, kwa nini uyakumbatie matiti
ya mwanamke mgeni? 21 Yehova huona kila kitu afanyacho mtu na huangalia mapito
yake yote. 22 Mtu mwovu atatekwa na makosa yake mwenyewe; kamba za dhambi
yake zitamnasa kwa nguvu. 23 Atakufa kwa kukosa maonyo; atapotelea mbali kwa
upumbavu wake wingi.

# 6

1 Mwanangu, kama utaweka pesa zako kuwa dhamana kwa mkopo wa jirani yako;
kama ukitoa ahadi yako katika mkopo wa mtu usiyemjua, 2 basi umejiwekea mtego
mwenyewe na umenaswa kwa maneno ya kinywa chako. 3 Mwanagu, ukinaswa kwa
maneno yako mwenyewe, fanya haya ili kujiokoa, kwa kuwa umeangukia kwenye
mikono ya jirani yako; nenda unyenyekee na ufanye shauri mbele ya jirani yako.
4 Usiruhusu usingizi katika macho yako wala kope za macho yako kusinzia. 5 Jiokoe
mwenyewe kama swala kutoka katika mkono wa mwindaji, kama ndege kutoka
katika mkono wa mwinda ndege. 6 Wewe mtu mvivu, mwangalie mchwa, zitafakari
njia zake ili kupata busara. 7 Hana akida, afisa au mtawala, 8 lakini huandaa chakula
chake wakati wa joto na wakati wa mavuno huweka hazina ili kula baadaye. 9 Ewe
mtu mvivu, utalala hata lini? Wakati gani utainuka usingizini?” 10 Lala kidogo, sizia
kidogo, kunja mikono kupumzika kidogo” - 11 ndipo umasikini wako utakapokujia
kama mporaji na uhitaji wako kama askari wa vita. 12 Mtu asiyefaa-mtu mwovu-
huishi kwa kauli za udanganyifu wake, 13 akipepesa macho yake, akiashilia kwa
miguu yake na kusonta kwa videle vyake. 14 Hufanya njama za uovu kwa hila ya
moyo wake; daima huchochea faraka. 15 Kwa hiyo msiba wake utamkumba kwa
ghafula, punde atavunjika vibaya wala hatapona. 16 Kuna vitu sita ambavyo Yehova
huvichukia, saba ambavyo ni chukizo kwake. 17 Macho ya mtu mwenye kiburi, ulimi
wa uongo, mikono inayomwaga damu ya watu maasumu, 18 moyo unaobuni njama
mbaya, miguu inayokimbilia maovu upesi, 19 shahidi asemaye uongo na apandaye
faraka kati ya ndugu. 20 Mwanangu, itii amri ya baba yako na wala usiyaache
mafundisho ya mama yako. 21 Uyafunge katika moyo wako siku zote; yafunge
kwenye shingo yako. 22 utembeapo, yatakuongoza; ulalapo yatakulinda, na uamkapo
yatakufundisha. 23 Maana amri ni taa, na mafundisho ni nuru; kinga za kuadilisha
za njia ya uzima. 24 Yanakulinda dhidi ya mwanamke malaya, dhidi ya maneno laini
ya uzinzi. 25 Moyoni mwako usiutamani uzuri wake wala usitekwe katika kope zake.
26 Kulala na malaya inaweza kugharimu bei ya kipande cha mkate, lakini mke wa
mtu mwingine inagharimu uzima wako wote. 27 Je mtu anaweza kubeba moto katika
kifua chake bila kuuguza mavazi yake? 28 Je mtu anaweza kutembea juu ya makaa
bila kuchomwa miguu yake? 29 Ndivyo alivyo mtu alalaye na mke wa jirani yake; yule
alalaye na huyo mke hatakosa adhabu. 30 Watu hawawezi kumdharau mwizi kama
anaiba ili kukidhi hitaji lake la njaa. 31 Walakini akimatwa, atalipa mara saba ya kile
alichoiba; lazima atoe kila kitu cha thamani katika nyumba yake. 32 Mtu anayefanya
uzinzi hana akili; hufanya hiyo kwa uharibifu wake mwenyewe. 33 Anasitahili aibu
na majeraha na fedheha yake haiwezi kuondolewa. 34 Maana vivu humghadhibisha

mtu; hatakuwa na huruma wakati wa kulipa kisasi chake. [35] Ujapompa zawadi nyingi,
hatakubali mbadala wa kusuruhishwa wala kulipwa.

## 7

[1] Mwanangu, yatunze maneno yangu na ndani yako udhihifadhi amri zangu.
[2] Uzilinde amri zangu ili uishi na uyatunzetu mafundisho yangu kama mboni ya
jicho. [3] Uyafunge katika vidole vyako; uyaandike katika kibao cha moyo wako.
[4] Mwambie hekima, "wewe ni dada yangu," na ufahamu mwite jamaa yako, [5] ili
ujitunze mwenyewe dhidi ya mwanake haramu, dhidi ya mwanamke mgeni mwenye
maneno laini. [6] Nilikuwa naangalia kwenye wavu wa dirisha la nyumba yangu.
[7] Nikawatazama watu mwenye ukosefu wa uzoefu, na miongoni mwa watu vijana
nikamwona kijana asiye na akili. [8] Kijana huyo alishuka mtaani kwenye kona karibu
na yule mwanamke, akaenda kwenye nyumba yake. [9] Ilikuwa katika utusiutusi wa
siku muda wa jioni, wakati wa usiku na giza. [10] Akakutana na yule mwanake, amevaa
kama kahaba, katika moyo wa udanyanyifu. [11] Alikuwa na kelele na upotovu; miguu
yake haikutulia kwenye masikani. [12] Alielekea mitaani, kisha sehemu ya sokoni, na
katika kila upande alisubiri kwa kuviza. [13] Basi akamshika na kumbusu, kwa uso
wa nguvu akamwambia, [14] leo nimetoa sadaka yangu ya amani, nimelipa nadhili
yangu, [15] hivyo nilikuja kukutana nawe, kuutafuta uso wako kwa hamu, na sasa
nimekupata. [16] Nimeweka matandiko juu ya kitanda changu, kitani za rangi kutoka
Misri. [17] Kitanda changu nimenyunyizia manemane, udi na mdalasini. [18] Njoo,
tunywe tujishibishe kwa upendo wetu hata asubuhi; tupate furaha kuu kwa matendo
ya mahaba. [19] Maana mume wangu hayupo nyumbani kwake; amekwenda safari ya
mbali. [20] Alichukua mkoba wa fedha; atarudi siku ya mwezi mpevu. [21] katika maneno
yake mengi akamshinda; na kwa midomo yake laini anampotosha. [22] Ghafula
alimfuata kama maksai anayekwenda kwa mchinjaji, kama ayala aliyekamatwa
kwa nguvu, [23] mpaka mshale upasue ini lake. Alikuwa kama ndege anayekimbili
kwenye mtego. Hakujua kuwa itamgharimu maisha yake. [24] Na sasa, wanangu,
nisikilizeni; zingatieni maneno ya kinywa changu. [25] Moyo wako usiyageukie mapito
yake; usipotoshwe katika mapito yake. [26] Amesababisha watu wengi kuanguka kwa
kuwajeruhi; ameua watu wengi. [27] Nyumba yake ipo juu ya barabara ya kwenda
kuzimu; huelekea chini kwenye vyumba vya mauti.

## 8

[1] Je hekima haiti? Je ufahamu hapazi sauti yake? [2] Juu ya kilima kando ya barabara,
kwenye njia panda, hekima anasimama. [3] Kando ya njia ya kuingilia mjini, karibu na
milango ya mji, anaita kwa sauti. [4] Watu, ninawaita ninyi na ninapaza sauti yangu
kwa wana wa wanadamu. [5] Ninyi wajinga, jifunzeni hekima, na ninyi mnaochukia
maarifa, lazima mjipatieni moyo wa ufahamu. [6] Sikiliza na mimi nitasema mambo
mazuri na nifumbuapo midomo yangu nitaongea haki. [7] Maana kinywa changu
hunena uaminifu na midomo yangu huchukia uovu. [8] Maneno ya kinywa changu yote
ni haki; hakuna kilichogeuzwa wala kupotoshwa. [9] Maneno yangu yote yamenyooka
kwa yule mwenye kuelewa; maneno yangu ni haki kwa wale wanaotafuta maarifa.
[10] Chagua fundisho langu badala ya fedha na maarifa kuliko dhahabu safi. [11] Maana
mimi, hekima ni bora kuliko vito; hakuna unachokitamani kinaweza kulinganishwa
na mimi. [12] Mimi, hekima, naishi kwa utaratibu, na ninamiliki maarifa na busara.
[13] Hofu ya Mungu ni kuchukia uovu- nachukia majivuno na kiburi, njia ya uovu,
na kauli iliyopotoka- hivyo ninavichukia. [14] Ninaushauri mzuri na hekima sahihi;
mimi ni busara; nguvu zipo kwangu. [15] Kwa njia yangu wafalme hutawala- pia
na waungwana, na wote ambao hutawala kwa haki. [16] Kwa njia yangu wafalme

hutawala na waungwana na wote wanaotawala kwa haki. 17 Nawapenda wale
wanaonipenda, na wale wanaonitafuta kwa bidii, wataniona. 18 Kwangu kunautajiri
na heshima, utajiri wa kudumu na haki. 19 Tunda langu ni bora kuliko dhahabu, bora
hata kuliko dhahabu safi. 20 Ninazalisha kilicho bora kuliko fedha safi. Natembea
katika njia ya haki, 21 katika mapito ambayo huelekea kwenye haki, ili niwape urithi
wale wanaonipenda na kuzijaza hazina zao. 22 Yehova aliniumba tokea mwanzo-
mwazoni mwa matendo yake ya nyakati za kale. 23 Tokea enzi za kale niliwekwa
katika nafasi- tokea kwanza, tokea mwanzo wa dunia. 24 Kabla ya bahari, mimi
nilizaliwa- kabla ya kuwepo chemchemi zenye maji tele. 25 Kabla ya milima na vilima
kuwekwa, mimi nilizaliwa. 26 Nilizaliwa kabla ya Yehova hajaiumba dunia wala
makonde, hata mavumbi ya kwanza katika dunia. 27 Nilikuwepo alipoziimarisha
mbingu, wakati alipochora mstari katika sura ya kilindi. 28 Nilikuwepo alipoimarisha
anga la juu na wakati wa kutengeneza kina cha chemchemi. 29 Nilikuwepo
alipotengeneza mipaka ya bahari, ili maji yasisambae kuvuka pale alipoyaamuru, na
wakati anaamuru misingi ya dunia sehemu ya kukaa. 30 Nilikuwa kando yake, kama
fundistadi mkuu, na mimi nilikuwa furaha yake siku kwa siku, nikifurahi mbele
zake daima. 31 Nilikuwa nikifurahi katika dunia yake yote na furaha yangu ilikuwa
kwa wana wa wanadamu. 32 Na sasa, wanangu, nisikilizeni, maana wale wazishikao
njia zangu watakuwa na furaha. 33 Sikilizeni fundisho langu na mpate hekima;
wala msilipuuze. 34 Anisikilizaye atakuwa na furaha- kila siku akitazama katika
malango yangu, akinisubiri pembeni mwa milango ya masikani yangu. 35 Maana
yeyote anionaye mimi, anapata uzima, naye atapata kibali kwa Yehova. 36 Na yeyote
asiyeniona mimi, hujiumiza mwenyewe, wote wanaonichukia hupenda mauti.

# 9

1 Hekima amejenga nyumba yake; amechonga nguzo saba kutoka katika miamba.
2 Ameandaa wanyama wake kwa chakula cha usiku; ameichanganya divai yake; na
kuandaa meza yake. 3 Amewatuma watumishi wake kupeleka mialiko na kutoka
mahali pa juu sana kwenye mji anaita: 4 "Wale wasiofunzwa waje hapa!" anawaam-
bia wale wasionaufahamu. 5 Njoo, ule chakula, na unywe divai nimeshaichanganya.
6 Acheni njia zenu za kijinga, na mkaishi; tembeeni katika njia ya ufahamu. 7 Yeyote
amrekebishaye mwenye dhihaka hukaribisha matusi na yeyote anayemshutumu
mtu mbaya atapata madhara. 8 Usimshutumu mwenye dhihaka, ama atakuchukia;
mshutumu mtu mwenye busara, naye atakupenda. 9 Mpe mafundisho mtu mwenye
busara, naye atakuwa na busara zaidi; mfundishe mtu mwenye haki, naye ataongeza
elimu. 10 Hofu ya Mungu ni chanzo cha hekima na maarifa ya Mtakatifu ni ufahamu.
11 Maana kwa njia yangu siku zako zitazidishwa na uzima wako utaongezewa miaka.
12 Kama unahekima, unahekima kwako mwenyewe, lakini ukidharau, utaibeba
peke yako. 13 Mwanamke mpumbavu anakelele nyingi- hajafunzwa wala haelewi
chochote. 14 Anakaa kwenye mlango wa nyumba yake, kwenye kiti cha sehemu ya
juu sana ya mji. 15 Anawaita kwa sauti wanaopita karibu, watu wale wanaotembea
wima katika njia zao. 16 Wale ambao hamjafunzwa njoni hapa ndani!" anawaambia
wale wasio na akili. " 17 Maji ya kuiba ni matamu na mkate unaoliwa kwa siri
unapendeza." 18 Lakini hajui kwamba wafu wapo pale, wageni wake wapo kwenye
vina vya kuzimu.

# 10

1 Mithali za Sulemani. Mwana mwenye hekima humfurahisha baba yake lakini
mwana mpumbavu huleta majonzi kwa mama yake. 2 Hazina zilizolimbikizwa kwa
uovu hakosa thamani, bali kwa kutenda haki hujilinda mbali na kifo. 3 Yehova

hawaachi wale watendao haki wapate njaa, bali hamu ya waovu huizuia. 4 Mkono
mlegevu humfanya mtu awe masikini, bali mkono wa mtu mwenye bidii hupata
utajiri. 5 Mwana mwenye busara hukusanya mazao wakati wa kiangazi, bali ni aibu
kwake alalaye wakati wa mavuno. 6 Zawadi kutoka kwa Mungu zipo juu ya kichwa
cha wale watendao haki; bali kinywa cha uovu hufunikwa kwa jeuri. 7 Mtu atendaye
haki anatufurahisha tunapomkumbuka, bali jina la mwovu litaoza. 8 Wale wenye
akili hukubali maagiza, bali mpumbavu mwenye maneno mengi ataangamia. 9 Yeye
anayetembea katika uadilifu hutembea katika usalama, bali yule anayepotosha njia
zake, ataonekana. 10 Yeye ambaye hukonyeza kwa jicho lake huleta majonzi, bali
mpumbavu mwenye maneno mengi atatupwa chini. 11 Kinywa cha mwenye kutenda
haki ni kama chemchemi ya maji ya uzima, bali kinywa cha uovu hufunikwa kwa
jeuri. 12 Chuki huchochea mafarakano, bali upendo hufunika juu ya makwazo yote.
13 Hekima inapatikana kwenye kinywa cha mtu mwenye ufahamu, bali fimbo ni kwa
ajili ya mgongo wa yule asiye na akili. 14 Watu wenye hekima hutunza maarifa, bali
kinywa cha mpumbavu huleta uharibifu karibu. 15 Mali ya mtu tajiri ni mji wake
mwenye ngome; ufukara wa masikini ni uharibifu wao. 16 Mshahara wa watenda
haki huelekea kwenye uzima; manufaa ya waovu huelekea dhambini. 17 Kuna njia
kwenda kwenye uzima kwa yule anayefuata maongozo, bali anayekataa maonyo
hupotea. 18 Yeye afichaye chuki anamidomo ya uongo, na yeye anayesambaza kashfa
ni mpumbavu. 19 Katika maneno mengi, hapakosi uhalifu, bali aliyemwangalifu
katika usemi wake ni mwenye busara. 20 Ulimi wa yule atendaye haki ni fedha
safi; kuna thamani ndogo katika moyo wa mbaya. 21 Midomo ya yule atendaye haki
huwastawisha wengi, bali wapumbavu hufa kwa sababu ya kukosa akili. 22 Zawadi
njema za Yehova huleta utajiri na haweki maumivu ndani yake. 23 Uovu ni mchezo
achezao mpumbavu, bali hekima ni furaha kwa mtu mwenye ufahamu. 24 Hofu ya
mwenye uovu humkumba ghafla, bali shauku ya mwenye haki itatimizwa. 25 Waovu
ni kama dhoruba inayopita, na hawapo tena, bali mwenye haki ni msingi unaodumu
milele. 26 Kama siki kwenye meno na moshi kwenye macho, ndivyo alivyo mvivu kwa
wale waliomtuma. 27 Hofu ya Yehova huongeza maisha, bali miaka ya waovu itakuwa
mifupi. 28 Matumaini ya wale watendao haki ndiyo furaha yao, bali miaka ya waovu
itakuwa mifupi. 29 Njia ya Yehova huwalinda wale wenye uadilifu, bali kwa waovu
ni uhalibifu. 30 Wale watendao haki hawataondolewa, bali waovu hawatabaki katika
nchi. 31 Katika kinywa cha wale watendao haki hutoka tunda la hekima, bali ulimi wa
kupotosha utakatwa. 32 Midomo ya wale watendao mema huyajua yanayokubalika,
bali kinywa cha waovu, huyajua yanayopotosha.

# 11

1 Yehova huchukia vipimo ambavyo havipo sahihi, bali hufurahia uzani dhahiri.
2 Kinapokuja kiburi, ndipo aibu huja, bali unyenyekevu huleta hekima. 3 Uadilifu
wa wenye haki huwaongoza, bali udanganyifu wa njia za wajanja utawaangamiza.
4 Utajiri hauna thamani siku ya ghadhabu, bali kwa kutenda haki hujilinda na
mauti. 5 Mwenendo wa mtu mwema huinyosha njia yake, bali waovu wataanguka
kwa sababu ya uovu wao. 6 Mwenendo mwema wa wale wampendezao Mungu
utawalinda salama, bali wadanganyifu hunaswa katika shauku zao. 7 Mtu mwovu
anapokufa, tumaini lake hupotea na tumaini lililokuwa katika nguvu zake linakuwa
si kitu. 8 Yule atendaye haki hulindwa katika taabu na badala yake taabu humjia
mwovu. 9 Kwa kinywa chake asiyeamini Mungu humwangamiza jirani yake, bali
kwa maarifa wale watendao haki hulindwa salama. 10 Wanapofanikiwa watendao
haki, mji hufurahi, waovu wanapoangamia, kunakuwa na kelele za furaha. 11 Kwa
zawadi nzuri za wale wanaompendeza Mungu, mji unakuwa mkubwa; kwa kinywa

cha waovu mji huvurugwa. 12 Mtu mwenye dharau kwa rafiki yake hana akili, bali
mtu mwenye ufahamu hunyamaza. 13 Anayekwenda akizunguka kwa kukashifu
hufunua siri, bali mtu mwaminifu hustiri jambo. 14 Pasipokuwa na uongozi
wenye busara, taifa huanguka, bali ushindi huja kwa kushauriana washauri wengi.
15 Anayemdhamini mkopo wa mgeni ataumia kwa usumbufu, bali anayechukia
kutoa rehani kwa namna ya ahadi yupo salama. 16 Mwanamke mwenye rehema
hupata heshima, bali watu wakorofi hufumbata utajiri. 17 Mtu mkarimu hufaidika
mwenyewe, bali mkatili hujiumiza mwenyewe. 18 Mtu mwovu husema uongo kupata
mishahara yake, bali yeye apandaye haki anavuna mishahara ya kweli. 19 Mtu
mwaminifu atendaye haki ataishi, bali yeye atendaye uovu atakufa. 20 Yehova
anawachukia wenye ukaidi mioyoni, bali anawapenda wale ambao njia zao hazina
makosa. 21 Uwe na uhakika juu ya hili- watu waovu hawatakosa adhabu, bali uzao
wa wale watendao haki watawekwa salama. 22 Kama pete ya dhahabu kwenye
pua ya nguruwe ndiyo alivyo mwanamke mzuri asiye na busara. 23 Shauku ya
wale watendao haki ni matokeo mema, bali watu waovu wanaweza kutumainia
ghadhabu tu. 24 Kuna yule ambaye hupanda mbegu- atakusanya zaidi; mwingine
hapandi- huyo anakuwa masikini. 25 Mtu mkarimu atafanikiwa na yule awapaye
maji wengine atapata maji yake mwenyewe. 26 Watu wanamlaani mtu ambaye
hukataa kuuza nafaka, bali zawadi njema hufunika kichwa chake ambaye huuza
nafaka. 27 Yule ambaye hutafuta mema kwa bidii pia anatafuta kibali, bali yule
atafutaye ubaya atapata ubaya. 28 Wale wanaotumaini utajiri wataanguka, bali kama
jani, wale watendao haki watasitawi. 29 Yule ambaye analeta taabu kwenye kaya
yake atairithi upepo na mpumbavu atakuwa mtumishi wa wenye moyo wa hekima.
30 Wale watendao haki watakuwa kama mti wa uzima, lakini vurugu huondoa uzima.
31 Tazama! Ikiwa wale watendao haki hupokea wanachositahili, je si zaidi kwa waovu
na wenye dhambi!

## 12

1 Anayependa mafundisho hupenda maarifa, bali yule anayechukia maonyo ni
mpumbavu. 2 Yehova humpa fadhila mtu mwema, bali mtu ambaye hufanya mipango
ya ufisada atahukumiwa. 3 Mtu hawezi kuimarishwa kwa uovu, bali wale watendao
haki hawawezi kung'olewa. 4 Mke mwema ni taji ya mume wake, bali yule aletaye
aibu ni kama ugonjwa unaoozesha mifupa yake. 5 Mipango ya wale watendao
haki ni adili, bali shauri la mwovu ni udanganyifu. 6 Maneno ya watu waovu
ni uviziaji unaosubiri nafasi ya kuua, bali maneno ya mwenye haki yatawatunza
salama. 7 Watu waovu wametupwa na kuondolewa, bali nyumba ya wale watendao
haki itasimama. 8 Mtu husifiwa kwa kadri ya hekima yake, bali yule anayechagua
ukaidi hudharauliwa. 9 Bora kuwa na cheo duni- kuwa mtumishi tu- kuliko kujisifu
kuhusu ukuu wako bila kuwa na chakula. 10 Yule atendaye haki anajali mahitaji
ya mnyama wake, bali huruma ya mwovu ni ukatili. 11 Yule atendaye kazi katika
shamba lake atapata chakula tele, bali anayesaka miradi duni hana akili. 12 Watu
waovu hutamani wanavyoiba watu wabaya kutoka kwa wengine, bali tunda la wale
watendao haki hutoka kwao mwenyewe. 13 Mtu mbaya hunaswa kwa maongezi yake
mabaya, bali wale watendao haki hujinasua katika taabu. 14 Mtu hushiba vitu vyema
kutokana na tunda la maneno yake, kama vile kazi ya mikono yake inavyompa
thawabu. 15 Njia ya mpumbavu ni sawa machoni pake mwenyewe, bali mtu wa
hekima husikiliza ushauri. 16 Mpumbavu huonyesha hasira yake papo hapo, bali
asiyejali tusi ni mwenye busara. 17 Asemaye ukweli huongea ilivyo haki, bali shahidi
wa uongo huongea uongo. 18 Maneno yake asemaye kwa pupa ni kama kurusha
upanga, bali ulimi wa mwenye hekima huleta uponyaji. 19 Midomo yenye kweli

itadumu milele, bali ulimi wa uongo ni kwa kitambo kidogo tu. 20 Kuna udanganyifu
katika mioyo ya wale wanaopanga kutenda uovu, bali furaha hutoka kwa washauri
wa amani. 21 Hakuna ugonjwa utakaowajia wale watendao haki, bali watu waovu
watajazwa matatizo. 22 Yehova anachukia midomo ya uongo, bali wale ambao huishi
kwa uaminifu ndiyo furaha yake. 23 Mtu mwenye busara anasitiri maarifa yake,
bali moyo wa wapumbavu hupiga yowe za kipumbavu. 24 Mkono wa mwenye bidii
utatawala, bali watu wavivu watawekwa katika kazi za kulazimishwa. 25 Mashaka
katika moyo wa mtu humwelemea, bali neno zuri humfurahisha. 26 Mwenye haki ni
kiongozi kwa rafiki yake, bali njia ya waovu huwaongoza katika kupotea. 27 Watu
wavivu hawawezi kubanika mawindo yao wenyewe, bali mtu wenye bidii atapata
mali zenye thamani. 28 Wale ambao wanatembea katika njia ya haki wanapata uzima
na katika mapito hayo hakuna kifo.

# 13

1 Mwana mwenye hekima husikia mafundisho ya baba yake, bali mwenye dhihaka
hatasikiliza karipio. 2 Mtu hufurahia vitu vizuri kutokana na matunda ya kinywa
chake, bali hamu ya wadanganyifu ni jeuri. 3 Yeye anayelinda kinywa chake
huyalinda maisha, bali anayefumbua sana midomo yake atajiangamiza mwenyewe.
4 Hamu ya watu wavivu ni uchu lakini hawapati kitu, bali hamu ya watu wenye bidii
hutoshelezwa sana. 5 Atendaye haki huchukia uongo, bali mtu mwovu hukinzana
mwenyewe, na kufanya ya kuaibisha. 6 Wenye haki huwalinda wale ambao ni
wakamilifu katika mapito yao, bali uovu huwaangusha wale watendao dhambi.
7 Kuna mtu ambaye hujitajirisha mwenyewe, lakini hana chochote na kuna mtu
ambaye hutoa kila kitu, bado ni tajiri kweli. 8 Mtu tajiri anaweza kufidia maisha
yake kwa mali zake, bali mtu masikini hatapokea kitisho cha aina hiyo. 9 Mwanga
wa mtu atendaye haki hufurahia, bali taa ya waovu itazimika. 10 Kiburi huzaa
mafarakano, bali kwa wale wasikiao shauri jema kuna hekima. 11 Penye majivuno
mengi utajiri hufifia, bali yeye apataye pesa kwa kufanya kazi kwa mkono wake
pesa zake zitaongezeka. 12 Tumaini linapoachwa, huvunja moyo, bali kukamilishwa
kwa shauku ni mti wa uzima. 13 Yule ambaye anadharau fundisho bado atakuwa
chini ya utawala wake, bali yeye ambaye anaheshimu amri atapewa thawabu.
14 Mafundisho ya mtu mwenye hekima ni chemchemi ya uzima, yanakuondoa kutoka
kwenye mitego ya mauti. 15 Busara njema huleta fadhila, bali njia ya wadanganyifu
haina mwisho. 16 Watu wenye busara hutenda kwa maarifa kwa kila uamuzi,
bali mpumbavu huonyesha upuuzi wake. 17 Mjumbe mbaya huangukia kwenye
shida, bali balozi mwaminifu huleta upatanisho. 18 Yeye ambaye hupuuza kurudiwa
atapata umasikini na aibu, bali heshima itamjia yeye ambaye hujifunza kutokana
na masahihisho. 19 Shauku iliyotambuliwa ni tamu kwa hamu, bali wapumbavu
huchukia kuacha uovu. 20 Tembea pamoja na watu wenye hekima nawe utakuwa na
hekima, bali rafiki wa wapumbavu atateseka. 21 Maafa huwakimbilia wenye dhambi,
bali wale watendao haki hupewa thawabu kwa mema. 22 Mtu mwema huacha
urithi kwa wajukuu wake, bali mali ya mwenye dhambi huwekwa akiba kwa yule
atendaye haki. 23 Shamba la masikini lisilolimwa linaweza huzalisha chakula kingi,
bali huchukuliwa kwa udhalimu. 24 Yeye ambaye hamrudi mwanawe humchukia,
bali yule anayempenda mwanawe humjali kwa kumwadibisha. 25 Yeye atendaye haki
hula hadi kutosheleza hamu yake bali tumbo la mwovu linanjaa daima.

# 14

1 Mwanamke mwenye busara huijenga nyumba yake, bali mwanamke mpumbavu
huibomoa kwa mikono yake mwenyewe. 2 Yeye aendaye kwa uaminifu humcha

Yehova, bali mkaidi humdharau katika njia zake. 3 Katika kinywa cha mpumbavu
hutoka chipukizi la kiburi chake, bali midomo ya wenye busara itawalinda. 4 Pale
pasipo na mifugo hori la kulishia ni safi, bali mazao mengi huweza kupatikana
kwa nguvu za maksai. 5 Shahidi mwaminifu hasemi uongo, bali shahidi wa uongo
hupumua uongo. 6 Mwenye dharau hutafuta hekima na hakuna hata, bali maarifa
huja kwa urahisi kwa mwenye ufahamu. 7 Nenda mbali kutoka kwa mtu mpumbavu,
maana hutapata maarifa kwenye midomo yake. 8 Hekima ya mtu mwenye busara
ni kuifahamu njia yake mwenyewe, bali upuuzi wa wapumbavu ni udanganyifu.
9 Wapumbavu hudharau wakati sadaka ya hatia inapotolewa, bali miongoni mwao
waaminifu hushiriki fadhila. 10 Moyo unayajua machungu yake mwenyewe na
hakuna mgeni anayeshiriki furaha yake. 11 Nyumba ya waovu itaangamizwa, bali
hema ya watu waaminifu itasitawi. 12 Kuna njia ambayo huonekana sawa kwa mtu,
lakini mwisho wake huelekea mauti tu. 13 Moyo unaweza kucheka lakini bado ukawa
katika maumivu na furaha inaweza kukoma ikawa huzuni. 14 Yule asiyemwaminifu
atapata anachostahili kwa njia zake, bali mtu mwema atapata kilicho chake. 15 Yeye
ambaye hakufundishwa huamini kila kitu, bali mtu mwenye hekima huzifikiria hatua
zake. 16 Mtu mwenye hekima huogopa na kutoka kwenye ubaya, bali mpumbavu
huliacha onyo kwa ujasiri. 17 Yeye ambaye anakuwa na hasira kwa haraka hufanya
mambo ya kipumbavu, na mtu anayefanya hila mbaya huchukiwa. 18 Wajinga hurithi
upumbavu, lakini watu wenye hekima wamezingirwa kwa maarifa. 19 Hao ambao ni
waovu watainama mbele yao walio wema na wale wenye uovu watasujudu kwenye
malango ya wenye haki. 20 Mtu masikini huchukiwa hata na marafiki zake, bali watu
matajiri wanamarafiki wengi. 21 Yeye ambaye huonyesha dharau kwa jirani yake
anafanya dhambi, bali yule ambaye huonyesha fadhila kwa masikini anafuraha. 22 Je
wale wanaofanya njama mbaya hawapotei? Bali wale wenye mpango wa kutenda
mema watapokea agano la uaminifu na udhamini 23 Katika kazi zote ngumu huja
faida, bali palipo na maongezi tu, huelekea kwenye umasikini. 24 Taji ya watu
wenye busara ni utajiri wao, bali upuuzi wa wapumbavu huwaletea upuu zaidi.
25 Shahidi mkweli huokoa maisha, bali shahidi wa uongo hupumua uongo. 26 Mtu
anapokuwa na hofu ya Yehova, pia anakuwa na matumaini zaidi ndani yake; vitu
hivi vitakuwa kama sehemu imara ya ulinzi kwa watoto wa mtu huyu. 27 Kumcha
Yehova ni chemchemi ya uzima, ili kwamba mtu aweze kujiepusha kutoka katika
mitego ya mauti. 28 Utukufu wa mfalme upo katika idadi kubwa ya watu wake, bali
pasipo watu mfalme huangamia. 29 Mtu mvumilivu anaufahamu mkubwa, bali mtu
mwepesi wa kuhamaki hukuza upuuzi. 30 Moyo wenye raha ni uzima wa mwili, bali
husuda huozesha mifupa. 31 Anayemkandamiza masikini humlaani Muumba wake,
bali anayeonyesha fadhila kwa wahitaji humtukuza yeye. 32 Mtu mwovu huangushwa
chini kwa matendo yake mabaya, bali mtu mwenye haki anakimbilio hata katika kifo.
33 Hekima hukaa katika moyo wa ufahamu, bali hata miongoni mwa wapumbavu
hujiachilia mwenyewe kwa kujulikana 34 Kutenda haki huliinua taifa, bali dhambi ni
chukizo kwa watu wowote. 35 Fadhila ya mfalme ni kwa mtumishi mwenye kutenda
kwa hekima, bali hasira yake ni kwa yule atendaye kwa kuaibisha.

# 15

1 Jawabu la upole huondoa ghadhabu, bali neno la ukatili huchochea hasira. 2 Ulimi
wa watu mwenye hekima husifu maarifa, bali kinywa cha wapumbavu humwaga
upuuzi. 3 Macho ya Yehova yapo kila mahali, yakiwatazama juu ya waovu na wema.
4 Ulimi unaoponya ni mti wa uzima, bali ulimi wa udanganyifu huvunja moyo.
5 Mpumbavu hudharau marudi ya baba yake, bali yeye anayejifunza kutokana na
masahihisho ni mwenye hekima. 6 Katika nyumba ya wale watendao haki kuna

hazina kubwa, bali mapato ya watu waovu huwapa taabu. 7 Midomo ya wenye
hekima husambaza maarifa, bali mioyo ya wapumbavu haifanyi hivyo. 8 Yehova
anachukia sadaka za watu waovu, bali maombi ya watu waadilifu ndiyo furaha yake.
9 Yehova anachukia njia ya watu waovu, bali anampenda yule ambaye huandama
haki. 10 Marudi ya ukatili hungojea kwa yeyote ambaye huiacha njia na yule
ambaye huchukia masahihisho atakufa. 11 Kuzimu na uharibifu vipo wazi mbele
za Yehova; je si zaidi sana mioyo ya wana wa wanadamu? 12 Mwenye mzaha
huchukia masahihisho; hatakwenda kwa wenye hekima. 13 Moyo wenye furaha
husababisha uchangamfu wa uso, bali huzuni huvunja moyo. 14 Moyo wa mwenye
ufahamu hutafuta maarifa, bali kinywa cha wapumbavu hujilisha kwenye upuuzi.
15 Siku zote za watu waliokandamizwa ni taabu, bali moyo wenye furaha unakaramu
daima. 16 Bora kitu kidogo pamoja na kumcha Mungu kuliko hazina kubwa pamoja
na ghasia. 17 Bora mlo wenye mboga kukiwa na upendo kuliko kuandaliwa ndama
aliyenona kwa chuki. 18 Mtu mwenye hasira huchochea mabishano, bali mtu ambaye
hukawia kukasirika hutuliza ugomvi. 19 Mapito ya mtu goigoi ni kama sehemu
yenye uwa wa miiba, bali mapito ya mtu mwadilifu ni njia kuu iliyojengwa imara.
20 Mwana mwenye busara huleta furaha kwa baba yake, bali mtu mpumbavu
humdharau mama yake. 21 Upuuzi humfurahia mtu ambaye amepungukiwa akili,
bali mwenye ufahamu hutembea katika njia nyofu. 22 Mipango huharibika ambapo
hakuna ushauri, bali washauri wengi wanafanikiwa. 23 Mtu anapata furaha wakati
anapotoa jibu la kufaa; je ni zuri kiasi gani neno kwa wakati muafaka! 24 Njia
ya uzima huwapeleka juu watu wenye hekima, ili waondoke kutoka chini kuzimu.
25 Yehova hurarua urithi wa mwenye kiburi, bali huzilinda mali za mjane. 26 Yehova
huyachukia mawazo ya watu waovu, bali maneno ya upole ni safi. 27 Mporaji huleta
shida kwenye familia yake, bali yeye ambaye huchukia rushwa ataishi. 28 Moyo
wa yule atendaye haki hutafakari kabla ya kujibu, bali kinywa cha watu waovu
humwanga ubaya wake wote. 29 Yehova yupo mbali na watu waovu, bali husikia
maombi ya wale watendao haki. 30 Nuru ya macho huleta furaha moyoni na habari
njema ni afya kwenye mwili. 31 Kama utazingatia wakati mtu anapokurekebisha
jinsi ya kuishi, utabaki miongoni mwa watu wenye busara. 32 Yeye anayekataa
karipio hujidharau mwenyewe, bali yule asikilizaye masahihisho hujipatia ufahamu.
33 Kumcha Yehova hufundisha hekima na unyenyekevu huja kabla ya heshima.

## 16

1 Mipango ya moyo ni ya mtu, bali Yehova hutoa jawabu kutoka kwenye ulimi wake.
2 Njia zote za mtu ni safi kwenye macho yake mwenyewe, bali Yehova huipima mioyo.
3 Kabidhi kwa Yehova kazi zako zote na mipango yako itafanikiwa. 4 Yehova alifanya
kila kitu kwa kusudi lake, hata waovu kwa ajili ya siku ya taabu. 5 Yehova anamchukia
kila mtu mwenye moyo wa majivuno, ingawa wanasimama imara, hawakosi kupata
adhabu. 6 Kwa agano la uaminifu na udhamini uovu husafishwa na kwa kumcha
Yehova watu hujitenga na ubaya. 7 Njia za mtu zinapompendeza Yehova, huwafanya
hata adui zake huyo mtu wawe na amani naye. 8 Bora kitu kidogo pamoja na haki,
kuliko mapato makubwa pamoja na udhalimu. 9 Katika moyo wake mtu hunuia njia
yake, bali Yehova huziongoza hatua zake. 10 Mshauri yupo katika midimo ya mfalme,
katika hukumu kinywa chake hakisemi kwa udanganyifu. 11 Vipimo vya kweli hutoka
kwa Yehova; uzito wote kwenye gunia ni kazi yake. 12 Wafalme wanapofanya mambo
maovu, hicho ni kitu cha kudharauliwa, kwa maana utawala huimarishwa kwa
kutenda haki. 13 Mfalme hufurahia midomo ambayo husema haki na anampenda
mwenye kusema waziwazi. 14 Hasira ya mfalme ni mjumbe wa mauti lakini mtu
mwenye busara atajaribu kutuliza hasira yake. 15 Katika nuru ya uso wa mfalme ni

uzima na fadhila yake ni kama wingu linaloleta mvua ya masika. 16 Ni bora kiasi
gani kupata hekima kuliko dhahabu. Kuchagua kupata ufahamu ni zaidi kuliko
fedha. 17 Njia kuu ya watu waadilifu hujitenga na ubaya; mwenye kuyahifadhi
maisha yake huilinda njia yake. 18 Kiburi hutangulia kabla ya uharibifu na moyo
wa kujivuna kabla ya maangamizi. 19 Ni bora kunyenyekea miongoni mwa watu
masikini kuliko kugawana ngawira pamoja watu wenye kiburi. 20 Mwenye kutafakari
yaliyofundishwa hupata kilicho chema na wenye kumtumaini Yehova watafurahi.
21 Mwenye hekima moyoni anaitwa ufuhamu na utamu wa hotuba huongeza uwezo
wa kufundisha. 22 Ufahamu ni chemchemi ya uzima kwake ambaye nayo, bali adhabu
ya wapumbavu ni upumbavu wao. 23 Moyo wa mtu mwenye hekima hutoa busara
katika kinywa chake na huongeza ushawishi katika midomo yake. 24 Maneno yenye
kufaa ni sega la asali -matamu kwenye nafsi na huponya mifupa. 25 Kuna njia ambayo
huonekana sawa kwa mtu, bali mwisho wake ni njia ya mauti. 26 Hamu ya kibarua
humfanyia kazi; njaa yake humsihi kuendelea. 27 Mtu duni huchimba madhara na
usemi wake ni kama moto unaounguza. 28 Mtu mkaidi huchochea mafarakano na
umbeya huwafarakanisha marafiki. 29 Mtu wa vurugu humdanganya jirani yake
na kumwongoza kwenye mapito ambayo si mema. 30 Yule anayekonyeza kwa jicho
anapanga njama za mambo ya ukaidi; wenye kuandama midomo yao watapitisha
mabaya. 31 Mvi ni taji ya utukufu; hupatikana kwa kuishi katika njia ya haki. 32 Ni
bora kukawia kuwa na hasira kuliko kuwa shujaa na mwenye kutawala roho yake
ni imara zaidi kuliko yule anayeuteka mji. 33 Kura hurushwa kwenye mkunjo, bali
maamuzi hutoka kwa Yehova.

# 17

1 Ni bora kuwa na utulivu pamoja chembe za mkate kuliko nyumba yenye sherehe
nyingi pamoja na ugomvi. 2 Mtumishi mwenye busara atatawala juu ya mwana
atendaye kwa aibu na atashiriki urithi kama mmoja wa ndugu. 3 Kalibu ni kwa fedha
na tanuu ni kwa dhahabu, bali Yehova huisafisha mioyo. 4 Mtu atendaye mabaya
huwasikiliza wale wanaosema maovu; muongo anausikivu kwa wale wanaosema
mambo mabaya. 5 Mwenye kumdhihaki masikini humtukana Muumba wake na
anayefurahia msiba hatakosa adhabu. 6 Wajukuu ni taji ya wazee na wazazi
huleta heshima kwa watoto wao. 7 Hotuba ya ushawishi haifai kwa mpumbavu;
kidogo zaidi midomo ya uongo inafaa kwa ufalme. 8 Rushwa ni kama jiwe la kiini
macho kwa yule ambaye atoaye; yeye anayeiacha, hufanikiwa. 9 Anayesamehe kosa
hutafuta upendo, bali yeye anayerudia jambo huwatenganisha marafiki wa karibu.
10 Karipio hupenya ndani ya mtu mwenye ufahamu kuliko mapigo mamia kwenda
kwa mpumbavu. 11 Mtu mbaya hutafuta uasi tu, hivyo mjumbe katiri atatumwa
dhidi yake. 12 Ni bora kukutana na dubu aliyeporwa watoto wake kuliko kukutana na
mpumbavu katika upumbavu wake. 13 Mtu anaporudisha mabaya badala ya mema,
mabaya hayatatoka katika nyumba yake. 14 Mwanzo wa mafarakano ni kama mtu
anayefungulia maji kila mahali, hivyo ondoka kwenye mabishano kabla ya kutokea.
15 Yeye ambaye huwaachilia watu waovu au kuwalaumu wale wanaotenda haki -
watu hawa wote ni chukizo kwa Yehova. 16 Kwa nini mpumbavu alipe fedha kwa
kujifunza hekima, wakati hana uwezo wa kujifunza? 17 Rafiki hupenda kwa nyakati
zote na ndugu amezaliwa kwa ajili ya nyakati za taabu. 18 Mtu asiyekuwa na akili
hufanya ahadi zenye mashariti na kuanza kuwajibika kwa madeni ya jirani yake.
19 Apendaye mafarakano anapenda dhambi; ambaye hutengeneza kizingiti kirefu
sana kwenye mlango wake husababisha kuvunjia kwa mifupa. 20 Mtu mwenye moyo
wa udanganyifu hapati chochote ambacho ni chema; na mwenye ulimi wa ukaidi
huanguka kwenye janga. 21 Mzazi wa mpumbavu huleta majonzi kwake mwenyewe;

baba wa mpumbavu hana furaha. 22 Moyo mchangamfu ni dawa njema, bali roho
iliyopondeka hukausha mifupa. 23 Mtu mwovu hukubali rushwa ya siri ili kupotosha
njia za haki. 24 Mwenye ufahamu huelekeza uso wake kwenye hekima, bali macho
ya mpumbavu huelekea ncha za dunia. 25 Mwana mpumbavu ni huzuni kwa baba
yake na uchungu kwa mwanamke aliyemzaa. 26 Pia, si vizuri kumwadhibu mwenye
kutenda haki; wala si vema kuwachapa mjeledi watu waadilifu wenye ukamilifu.
27 Mwenye maarifa hutumia maneno machache na mwenye ufahamu ni mtulivu.
28 Hata mpumbavu hudhaniwa kuwa na busara kama akikaa kimya; wakati anapokaa
amefunga kinywa chake, anafikiriwa kuwa na akili.

## 18

1 Yule ambaye hujitenga hutafuta matakwa yake mwenyewe na hupingana na
hukumu zote za kweli. 2 Mpumbavu hapati raha katika ufahamu, lakini hufunua kile
kilichopo katika moyo wake. 3 Mtu mwovu anapokuja, dharau huja pamoja naye-
sambamba na aibu na shutuma. 4 Maneno ya kinywa cha mtu ni maji yenye kina
kirefu; chemchemi ya hekima ni mkondo unaotiririka. 5 Si vema kuwa na upendeleo
kwa mwovu, wala haifai kukana haki kwa wale watendao mema. 6 Midomo ya
mpumbavu huletea mafarakano na kinywa chake hukaribisha mapigo. 7 Kinywa cha
mpumbavu ni uharibifu wake na hujinasa mwenye kwa midomo yake. 8 Maneno
ya mmbea ni kama chembe tamu na hushuka katika sehema za ndani sana kwenye
mwili. 9 Basi, ambaye ni mzembe katika kazi yake ni ndugu yake anayeharibu wengi.
10 Jina la Yehova ni mnara imara; atendaye haki hukimbilia na kuwa salama. 11 Mali
ya tajiri ni mji wake imara na katika fikira zake ni kama ukuta mrefu. 12 Moyo wa mtu
huwa na kiburi kabla ya anguko lake, bali unyenyekevu hutangulia kabla ya heshima.
13 Anayejibu kabla ya kusikiliza- ni upuuzi na aibu yake. 14 Roho ya mtu itajinusuru na
madhara, bali roho iliyopondeka nani anaweza kuivumilia? 15 Moyo wa mwenye akili
hujipatia maarifa na usikivu wa mwenye busara huitafuta. 16 Zawadi ya mtu inaweza
kufungua njia na kumleta mbele ya mtu muhimu. 17 Wa kwanza kujitetea katika
shitaka lake huonekana kuwa na haki hadi mpinzani wake aje na kumuuliza maswali.
18 Kupiga kura kunamaliza mabishano na kuwatawanya wapinzani imara. 19 Ndugu
aliyechukizwa ni mgumu kushawishiwa kuliko mji wenye nguvu, na kugombana ni
kama makomeo ya ngome. 20 Tumbo la mtu litashiba kutoka kwenye tunda la kinywa
chake; atatoshelezwa kwa mavuno ya midomo yake. 21 Uzima na kifo hutawaliwa
kwa ulimi, na wale wenye kuupenda ulimi watakula tunda lake. 22 Yeye apataye
mke anapata kitu chema na kupokea fadhila kutoka kwa Yehova. 23 Mtu masikini
huomba rehema, lakini mtu tajiri hujibu kwa ukali. 24 Anayejidai kwa marafiki wengi
watamleta katika uharibifu, bali yupo rafiki ambaye huwa karibu kuliko ndugu.

## 19

1 Bora mtu masikini ambaye huenenda katika uadilifu wake kuliko mwenye ukaidi
katika maneno yake na ni mpumbavu. 2 Tena, si vizuri kuwa na hamu bila maarifa
na mwenye kukimbia haraka sana hukosea njia. 3 Upuuzi wa mtu unaharibu maisha
yake na moyo wake hughadhabika dhidi ya Yehova. 4 Utajiri huongeza marafiki
wengi, bali mtu masikini hutengwa na rafiki zake. 5 Shahidi wa uongo hatakosa
adhabu na mwenye kupumua uongo hataokoka. 6 Wengi wataomba fadhila kutoka
kwa mtu mkarimu na kila mtu ni rafiki wa yule anayetoa zawadi. 7 Mtu masikini
huchukiwa na ndugu zake wote; je marafiki wengi kiasi gani hujitenga kutoka
kwake! Anawaita, lakini wameondoka. 8 Anayepata hekima huyapenda maisha
yake mwenyewe; yeye atunzaye ufahamu atapata kilicho chema. 9 Shahidi wa
uongo hatakosa kuadhibiwa, bali mwenye kupumua uongo ataangamia. 10 Haifai

kwa mpumbavu kuishi kwa anasa- wala kwa mtumwa kutawala juu ya wafalme.
[11] Busara humfanya mtu achelewe kukasirika na utukufu wake ni kusamehe kosa.
[12] Ghadhabu ya mfalme ni kama muungurumo wa simba kijana, bali fadhila yake
ni kama umande kwenye majani. [13] Mwana mpumbavu ni uharibifu kwa baba
yake na mke mgomvi ni maji yanayochuruzika daima. [14] Nyumba na utajiri ni
urithi kutoka kwa wazazi, bali mke mwenye busara hutoka kwa Yehova. [15] Uvivu
unamtupa mtu kwenye usingizi mzito, bali asiyetamani kufanya kazi atakwenda njaa.
[16] Yeye anayetii amri huyaongoza maisha yake, bali mtu asiyefikiri juu ya njia zake
atakufa. [17] Mwenye ukarimu kwa masikini humkopesha Yehova na atalipwa kwa
kile alichofanya. [18] Mrudi mwanao wakati kuna matumaini na usiwe na shauku
ya kumweka katika mauti. [19] Mtu mwenye hasira kali lazima alipe adhabu; kama
ukimwokoa, utafanya hivyo mara mbili. [20] Sikiliza ushauri na ukubali maelekezo,
ili uweze kuwa na hekima mwishoni mwa maisha yako. [21] Moyoni mwa mtu
kuna mipango mingi, bali kusudi la Yehova ndilo litakalo simama. [22] Shauku ya
mtu ni uaminifu na mtu masikini ni bora kuliko muongo. [23] Kumheshimu Yehova
huwaelekeza watu kwenye uzima; mwenye nayo atashibishwa na hatadhurika kwa
madhara. [24] Mtu goigoi huuzika mkono wake ndani ya dishi; hataurudisha juu ya
kinywa chake. [25] Kama utampiga mwenye mzaha, wajinga watakuwa na hekima;
mwelekeze mwenye ufahamu, naye atapata maarifa. [26] Anayempora baba yake
na kumfukuza mama yake ni mwana anayeleta aibu na shutuma. [27] Mwanangu,
kama utaacha kusikiliza maelekezo, utapotea kutoka kwenye maneno ya maarifa.
[28] Shahidi mpotofu huidhihaki haki na kinywa cha waovu humeza uovu. [29] Hukumu
ipo tayari kwa wenye dhihaka na mjeledi kwa migongo ya wapumbavu.

## 20

[1] Divai ni dhihaka na kinywaji kikali ni mgomvi; anayepotea kwa kunywa hana
busara. [2] Kumwogopa mfalme ni kama kumwogopa simba kijana aungurumaye,
yeyote anayemkasirisha hutoa fidia ya maish yake. [3] Ni heshima kwa mtu yeyote
kujiepusha na mafarakano, bali kila mpumbavu hurukia kwenye mabishano. [4] Mtu
mvivu halimi majira ya kipupwe; hutafuta mazao wakati wa mavuno lakini hapati
kitu. [5] Makusudi ndani ya moyo wa mtu ni kama maji yenye kina, bali mtu mwenye
ufahamu huyateka. [6] Mara nyingi mtu husema yeye ni mwaminifu, lakini ni nani
awezaye kumpata yule mwaminifu? [7] Mtu atendaye haki hutembea katika uaminifu
wake na wana wake wanaofuata baada yake wanafuraha. [8] Mfalme anayeketi
kwenye kiti cha hukumu akifanya kazi za kuhukumu hupembua kwa macho yake
mabaya yote yaliyoko mbele yake. [9] Nani anayeweza kusema, “Nimeuweka safi
moyo wangu; nipo huru na dhambi zangu”? [10] Mizani tofauti na vipimo visivyosawa
- Yehova huvichukia vyote. [11] Hata kijana hujulikana kwa matendo yake, kwa
mwenendo wake kama ni safi na uadilifu. [12] Masikio yanayosikia na macho
yanayoona- Yehova aliyafanya yote. [13] Usipende usingizi au utakuwa masikini;
fumbua macho yako na utakuwa na vyakula tele. [14] “Mbaya! Mbaya!” anasema
mnunuzi, lakini akiondoka anajisifu. [15] Ipo dhahabu na mawe ya thamani, lakini
midomo yenye maarifa ni kito cha thamani. [16] Chukua vazi kama mmiliki wake
ataweka fedha kama dhamana kwa deni la mgeni, na lichukue kama anaweka
dhamana kwa uzinifu. [17] Mkate uliopatikana kwa ulaghai unaladha tamu, lakini
baadaye kinywa chake kitajaa kokoto. [18] Mipango huimarishwa kwa ushauri na kwa
mwongozo wa busara utapigana vita. [19] Mmbea hufunua siri na kwa hiyo hupaswi
kushirikiana na watu ambao huongea sana. [20] Kama mtu atamlaani baba yake au
mama yake, taa yake itapulizwa katikati ya giza. [21] Urithi uliopatikana mwanzoni
kwa haraka utakuwa na mema kidogo mwishoni. [22] Usiseme “ Mimi nitakulipiza

kwa kosa hili" Msubiri Yehova na yeye atakuokoa. [23] Yehova huchukia mizani isiyo
sawa na vipimo vya udanganyifu si vizuri. [24] Hatua za mtu huongozwa na Yehova;
namna gani basi ataifahamu njia yake? [25] Ni mtego kwa mtu kusema kwa pupa, "
Kitu hiki ni kitakatifu" na kuanza kufikiri juu yake kwamba kina maana gani baada
ya kufanya kiapo. [26] Mfalme mwenye busara huwapepeta waovu na huligeuza juu
yao gurudumu la kupuria. [27] Roho ya mtu ni taa ya Yehova, hutafiti sehemu zake zote
za ndani kabisa. [28] Agano la uaminifu na udhamini humhifadhi mfalme; kiti chake
cha enzi hufanywa thabiti kwa upendo. [29] Utukufu wa watu vijana ni nguvu zao na
fahari ya watu wazee ni mvi zao. [30] Mapigo yanayoleta kidonda huusafisha ubaya
na vichapo hufanya sehemu za ndani kabisa kuwa safi.

# 21

[1] Moyo wa mfalme ni mfereji wa maji katika mkono wa Yehova; anaugeuza
popote anakopenda. [2] Kila njia ya mtu ni sawa katika macho yake mwenyewe,
lakini ni Yehova anayeipima mioyo. [3] Kutenda haki na adili hukubaliwa zaidi na
Yehova kuliko sadaka. [4] Macho ya kiburi na moyo wa majivuno- taa ya waovu- ni
dhambi. [5] Mipango ya mwenye juhudi huelekea kwenye mafanikio tu, bali kila mtu
anayetenda kwa haraka huelekea umasikini. [6] Kujipatia utajiri kwa ulimi wa uongo
ni mvuke unaopita upesi na mtego ambao unafisha. [7] Vurugu ya waovu itawaburuta
mbali, maana wanakataa kutenda haki. [8] Njia ya mwenye hatia ni ukatiri, bali
mwenye usafi hutenda yaliyo ya haki. [9] Bora kuishi kwenye kona ya juu darini kuliko
katika nyumba pamoja na mke mgonvi. [10] Hamu ya mwovu ni uchu wa mabaya;
jirani yake haoni ukarimu katika macho yake. [11] Mwenye dhihaka anapoadhibiwa
mjinga hupata busara, na mtu mwenye busara anapofundishwa, anaongeza maarifa.
[12] Atendaye haki huilinda nyumba ya mwovu; huwashusha waovu kwenye uharibifu.
[13] Anayeziba masikio yake kwenye kilio cha masikini, pia atalia, lakini hatajibiwa.
[14] Zawadi ya siri hutuliza hasira na zawadi ya kificho hutuliza ghadhabu kuu. [15] Haki
ikitendeka, huleta furaha kwa mwenye kutenda wema, lakini huleta hofu kubwa kwa
watenda mabaya. [16] Yule anayezurura kutoka kwenye njia ya ufahamu, atapumzika
kwenye kusanyiko la wafu. [17] Anayependa raha atakuwa masikini; anayependa
divai na mafuta hawezi kuwa tajiri. [18] Mtu mbaya ni fidia kwa yule atendaye haki,
na mdanganyifu ni fidia kwa waaminifu. [19] Bora kuishi jangwani kuliko kuishi
pamoja na mwanamke ambaye huchochea sana ugomvi na malalamiko. [20] Hazina
yenye thamani na mafuta vipo nyumbani kwa mwenye busara, bali mtu mpumbavu
huviharibu. [21] Mtu atendaye haki na mwema -huyu mtu hupata uzima, haki na
heshima. [22] Mtu mwenye busara huupima mji wa mashujaa, na huiangusha ngome
wanayoitumaini. [23] Anayelinda kinywa chake na ulimi wake hujilinda mwenyewe
na taabu. [24] Mtu mwenye kiburi na maringo- " Dhihaka" ndilo jina lake - hutenda
kwa majivuno na kujidai. [25] Shauku ya mtu mvivu itamuua, maana mikono yake
hukataa kufanya kazi. [26] Kwa siku nzima hupatwa na uchu na uchu zaidi, lakini
atendaye haki hutoa na wala hazuii. [27] Sadaka ya mwovu ni chukizo; huwa ni chukizo
zaidi anapoileta kwa nia mbaya. [28] Shahidi wa uongo ataangamia, bali anayesikiliza
ataongea kwa muda wote. [29] Mtu mwovu huufanya uso wake kuwa mgumu, bali mtu
mwadilifu ni thabiti juu ya njia zake. [30] Hakuna hekima, hakuna ufahamu, na hakuna
shauri linaloweza kusimama kinyume na Yehova. [31] Farasi hutayarishwa kwa siku
ya mapigano, lakini ushindi hupatikana kwa Yehova.

# 22

[1] Jina jema huchaguliwa dhidi ya utajiri mwingi na fadhila ni bora kuliko fedha
na dhahabu. [2] Watu matajiri na masikini wanafanana katika hili - Yehova ni

muumba wao wote. [3] Mtu mwenye hekima huiona taabu na kujificha mwenyewe,
bali mjinga huendelea mbele na huumia kwa ajili yake. [4] Thawabu ya unyenyekevu
na kumcha Yehova ni utajiri, heshima na uzima. [5] Miiba na mitego hulala katika
njia ya wakaidi; yeye anayelinda maisha yake atakuwa mbali navyo. [6] Mfundishe
mtoto njia inayompasa na wakati akiwa mzee hatayaacha mafundisho hayo. [7] Watu
matajiri huwatawala watu masikini na mwenye kukopa ni mtumwa wa yule
anayekopesha. [8] Yule anayepanda udhalimu atavuna taabu na fimbo ya hasira yake
itanyauka. [9] Mwenye jicho la ukarimu atabarikiwa, maana anashiriki mkate wake
pamoja na masikini. [10] Mfukuze mbali mwenye dhihaka, na ugomvi utaondoka,
mashindano na matukano yatakoma. [11] Anayependa moyo safi na mwenye maneno
ya neema, atakuwa rafiki yake mfalme. [12] Macho ya Yehova huyaangalia maarifa,
bali huyapindua maneno ya wadanganyifu. [13] Mtu mvivu husema, " Kuna simba
mtaani! Nitauwawa sehemu za njia." [14] Kinywa cha malaya ni shimo lenye kina
kirefu; hasira ya Yehova huchochewa dhidi ya yule anayetumbukia ndani yake.
[15] Upumbavu umefungwa katika moyo wa mtoto, lakini marudi ya fimbo huutoa.
[16] Anayewanyanyasa watu masikini ili kuongeza mali yake, au kuwapa matajiri,
atakuwa masikini. [17] Tega sikio lako na usikilize maneno ya wenye busara na utumia
moyo wako katika maarifa yangu, [18] maana itakuwa furaha kwako kama utayaweka
ndani yako, kama yote yatakuwa katika midomo yako. [19] Basi tumaini lako liwe
kwa Yehova, ninayafundisha kwako leo- hata kwako. [20] Sijakuandikia wewe misemo
thelathini ya mafundisho na maarifa, [21] kwa kukufundisha kweli katika maneno
haya yenye uaminifu, ili uwe na majibu yenye kutegemewa kwa waliokutuma?
[22] Usimwibie masikini kwa sababu ni masikini, au kumponda kwenye lango, [23] maana
Yehova ataitetea kesi yao, na atawaibia uzima wale waliowaibia masikini. [24] Usifanye
urafiki na mtu mwenye kutawaliwa na hasira na wala usiambatane pamoja na
mwenye hasira kali, [25] au utajifunza njia zake na utakuwa chambo kwa nafsi yako.
[26] Usiwe miongoni mwao wapigao mikono, mwenye kuahidi madeni. [27] Kama
umekosa njia za kulipa, nini kitaweza kuzuia mtu kuchukua kitanda chako chini
yako? [28] Usiondoe jiwe la mpaka la wahenga ambalo baba zako wameweka. [29] Je
umemwona mtu aliyeuwawa kwenye kazi yake? Atasimama mbele ya wafalme;
hatasimama mbele ya watu wa kawaida.

# 23

[1] Unapoketi kula pamoja na mtawala, angalia kwa uangalifu kilichopo mbele yako,
[2] na kama ni mtu unayependa kula chakula sana weka kisu kooni. [3] Usitamani
vinono vyake maana ni chakula cha uongo. [4] Usifanye kazi sana ili kupata mali;
uwe na busara ya kutosha ili ujue wakati wa kuacha. [5] Je utaruhusu macho
yako yaangaze juu yake? Itaondoka, maana itawaa mabawa kama tai na kuruka
angani. [6] Usile chakula cha yule mwenye jicho baya- na usiwe na shauku ya
vinono vyake, [7] maana ni mtu mwenye kuhesabu gharama ya chakula. "Kula na
kunywa!" anakuambia, lakini moyo wake haupo pamoja nawe. [8] Utatapika kiasi
kidogo ulichokula na utakuwa umepoteza sifa zako njema. [9] Usiongee katika usikivu
wa mpumbavu, maana atadharau hekima ya maneno yako. [10] Usihamishe jiwe la
mpaka wa kale au kunyang'anya mashamba ya yatima, [11] maana Mkombozi wao
ni imara na atatetea kesi yao dhidi yako. [12] Elekeza moyo wako katika mafundisho
na masikio yako kwenye maneno ya maarifa. [13] Usizuie kuadilisha mtoto, maana
ukimchapa kwa fimbo, hatakufa. [14] Ni wewe unayepaswa kumchapa kwa fimbo
na kuikoa nafsi yake kuzimu. [15] Mwanangu, kama moyo wako una busara, basi
moyo wangu utafurahi pia; [16] sehemu zangu ndani kabisa zitafurahi sana midomo
yako inaponena haki. [17] Usiruhusu moyo wako kuwahusudu wenye dhambi, lakini

endelea kumcha Yehova siku zote. [18] Hakika tumaini lako halitaondolewa na siku
zako za hapo baadaye. [19] Sikia- wewe! - mwanangu, na uwe mwenye busara na
uelekeze moyo wako katika njia. [20] Usishirikiane pamoja na walevi, au pamoja
na walaji wa nyama walafi, [21] maana mlevi na mlafi wanakuwa masikini na
usingizi utawavika kwa matambara. [22] Msikilize baba yako ambaye alikuzaa na
usimdharau mama yako wakati akiwa mzee. [23] Inunue kweli, lakini usiiuze; nunua
hekima, nidhamu, na ufahamu. [24] Baba yake mwenye haki atafurahia sana, na
yule amzaaye mtoto mwenye busara atamfurahia. [25] Mfurahishe baba yako na
mama yako na yule aliyekuzaa afurahie. [26] Mwanangu, nipe moyo wako na macho
yako yachunguze njia zangu. [27] Maana malaya ni shimo refu, na mke wa mume
mwingine ni kisima chembamba. [28] Anavizia kama mnyang'anyi na huongeza idadi
ya wadanganyifu miongoni mwa wanadamu. [29] Nani mwenye taabu? Nani mwenye
huzuni? Nani mwenye mapigano? Nani mwenye malalamiko? Nani mwenye
majeraha bila sababu? Nani mwenye macho mekundu? [30] Ni wale ambao huzengea
kwenye mvinyo, wale wanaojaribu kuchanganya mvinyo. [31] Usiutazame mvinyo
ukiwa mwekundu, wakati unametameta kwenye kikombe na kutelemka kwa uraini.
[32] Mwisho wake unauma kama nyoka na sumu yake kama kifutu. [33] Macho yako
yataona vitu vigeni na moyo wako utatamka vitu vya ukaidi. [34] Utakuwa kama
anayelala kwenye bahari au anayelala juu ya mlingoti. “ [35] Wamenipiga,” utasema,
“ lakini sikuumia. Wamenichapa, lakini sikuwa na hisia. Nitaamka lini? Nitatafuta
kinywaji kingine.”

# 24

[1] Usiwe na husuda kwa wenye ubaya, wala usitamani kuambatana nao, [2] kwa
sababu mioyo yao inapanga njama za vurugu na midomo ya huongea juu ya
madhara. [3] Kwa hekima nyumba hujengwa na kwa ufahamu huimarishwa. [4] Kwa
maarifa vyumba hujazwa vitu vyote vya thamani na utajiri wa kupendeza. [5] Shujaa
wa hekima ni imara, na mtu wa maarifa huongeza nguvu zake; [6] maana kwa
uongozi wa busara unaweza kufanya vita na kwa washauri wengi kuna ushindi.
[7] Hekima ipo juu sana kwa mpumbavu; hafumbui kinywa chake kwenye mlango.
[8] Kuna yule mwenye kupanga kufanya mabaya- watu wanamwita bwana wa
njama. [9] Mipango ya mpumbavu ni dhambi na watu humchukia mwenye dhihaka.
[10] Kama utakuwa dhaifu na mwenye kuogopa siku ya taabu, basi nguvu zako ni
haba. [11] Waokoe wanaochukuliwa kwenda kwenye mauti na uwashikilie wale
wanaopepesuka kwenda kwa mchinjaji. [12] Kama utasema, “Tazama, hatujui chochote
juu ya hili,” je yule anayepima mioyo hajui unachosema? Na yule anayelinda maisha
yako, je hajui? Je Mungu hatampa kila mmoja kile anachostahili? [13] Mwanangu,
kula asali kwa kuwa ni nzuri, kwa sababu matone ya sega la asali ni matamu
unapoonja. [14] Hekima ndiyo ilivyo katika nafsi yako - kama utaitafuta, tumaini
lako halitabatilika na kutakuwa na tumaini. [15] Usisubiri kwa kuvizia kama waovu
ambao hushambulia nyumba ya mwenye haki. Usiiharibu nyumba yake! [16] Maana
mwenye haki huanguka mara saba na kuinuka tena, lakini waovu huangushwa
kwa maafa. [17] Usisherekee wakati adui yako anapoanguka na wala moyo wako
usifurahi anapojikwaa, [18] au Yehova ataona na kutoridhika na kuondoa ghadhabu
juu yake. [19] Usifadhaike kwa sababu ya watenda mabaya, na wala usiwahusudu
watu waovu, [20] maana mtu mbaya hana matumaini na taa ya watu waovu itazimika.
[21] Mwanangu; mche Yehova, na umwogope mfalme, usishirikiane na watu wenye
kuasi dhidi yao, [22] maana kwa ghafula msiba wao utakuja na ni nani ajuaye ukubwa
wa uharibifu utakao kuja kutoka kwa hao wote? [23] Haya ni maneno ya wenye
busara pia. Upendeleo katika kuhukumu kesi kwa sheria si vizuri. [24] Anayemwambia

mwenye hatia, “ Wewe upo sawa,” atalaaniwa na watu na mataifa yatamchukia.
25 Bali wenye kuwakemea waovu watakuwa na furaha na zawadi za wema zitakuja
kwao. 26 Anayetoa jibu la kweli hutoa busu kwenye midomo. 27 Andaa kazi yako ya
nje, na tayarisha kila kitu kwa ajili yako mwenyewe shambani; baada ya hapo, jenga
nyumba yako. 28 Usitoe ushahidi dhidi ya jirani yako bila sababu na usidanganye kwa
midomo yako. 29 Usiseme, “ Mimi nitamtendea kile alichonitendea; nitalipiza kwa
kile alichofanya.” 30 Nilikwenda jirani na shamba la mtu mvivu, nikapita kwenye
shamba la mzabibu la mtu asiye na akili. 31 Miiba imeota kila sehemu, ardhi ilikuwa
imefunikwa kwa upupu, na ukuta wake wa mawe ulikuwa umebomoka. 32 Kisha
nikaliona na kufikiria juu yake; nikatazama na kupokea mafundisho. 33 Kulala
kidogo, kusinzia kidogo, kupumzika kwa kukunja mikono kidogo- 34 na umasikini
huja kwa kutembea juu yako, na mahitaji yako kama askari mwenye silaha.

# 25

1 Hizi tena ni mithali za Sulemani, zilinakiliwa na watu wa Hezekia, mfalme wa
Yuda. 2 Ni utukufu wa Mungu kuficha jambo, bali utukufu wa wafalme kutafiti
juu ya jambo. 3 Kama mbingu ni kwa kimo na dunia ni kwa kina, ndivyo hivyo
moyo wa wafalme hauchunguziki. 4 Ondoa takataka kutoka kwenye fedha na
mfua vyuma anaweza kutumia fedha katika ufundi wake. 5 Pamoja na hayo,
waondoe watu waovu mbele ya mfalme na kiti chake cha enzi kitaimarishwa kwa
kutenda haki. 6 Usijitukuze mwenyewe mbele ya mfalme na usisimame katika
sehemu iliyoteuliwa kwa watu wakuu. 7 Ni bora yeye akuambie, “Njoo hapa”
kuliko wewe kujiaibisha mbele ya mkuu. 8 Usiharakishe kufanya kuhukumu,
kwa kile ulichokishuhudia. Maana utafanya nini mwishoni, wakati jirani yako
atakapokuaibisha? 9 Jitetee kesi yako kati ya jirani yako na wewe na usifunue siri
ya mtu mwingine, 10 au vinginevyo anayekusikia ataleta aibu juu yako na taarifa
mbaya juu yako haiwezi kunyamazishwa. 11 Kunena maneno yenye kuchaguliwa
vizuri, ni kama nakshi za dhahabu iliyoungwa kwenye fedha. 12 Kama pete ya
dhahabu au kito kilichotengenezwa kwa dhahabu safi ndivyo lilivyo karipio la busara
kwenye sikio linalosikia. 13 Kama baridi ya theluji wakati wa mavuno ndivyo alivyo
mjumbe mwaminifu kwa wenye kumtuma; huyahifadhi maisha ya mabwana wake.
14 Kama mawingu na upepo bila mvua ndivyo alivyo mwenye kujisifu kuhusu zawadi
asiyoitoa. 15 Kwa uvumilivu mtawala anaweza kushawishiwa na ulimi raini unaweza
kuvunja mfupa. 16 Kama utapata asali, kula ya kutosha- vingenevyo, ukila nyingi
sana, utaitapika. 17 Usiweke mguu wako kwenye nyumba ya jirani yako mara nyingi,
anaweza kuchoshwa nawe na kukuchukia. 18 Mtu anayetoa ushuhuda wa uongo
dhidi ya jirani yake ni kama rungu lililotumiwa katika vita, au upanga, au mshale
mkali. 19 Kumtumaini mtu asiye mwaminifu wakati wa taabu ni kama jino bovu
au mguu unaoteleza. 20 Kama mtu anayevua nguo katika hali ya baridi, au kama
siki iliyotiwa kwenye magadi, ndivyo alivyo anayeimba wimbo kwa mwenye moyo
mzito. 21 Kama adui yako ana njaa, mpe chakula ale na kama ana kiu, mpe maji
ya kunywa, 22 maana utamwekea mkaa juu ya kichwa chake na Yehova atakupa
thawabu. 23 Ni hakika upepo wa kaskazini huleta mvua, ndivyo mtu anayesema siri
hufanya sura zikasirike. 24 Ni bora kuishi kwenye pembe ya darini kuliko kuchangia
nyumba pamoja na mwanamke mgomvi. 25 Kama maji ya baridi kwa mwenye kiu,
ndivyo ilivyo habari njema kutoka nchi ya mbali. 26 Kama chemchemi iliyochafuliwa
au kisima kilichoharibiwa ndivyo alivyo mtu mwema ambaye huyumbayumba mbele
ya watu waovu. 27 Si vema kula asali nyingi mno; hivyo ni kama kutafuta heshima
baada heshima. 28 Mtu bila kujitawala ni kama mji ulibomolewa na usiokuwa na
kuta.

# 26

1 Kama theluji wakati wa joto au mvua kwenye mavuno, ndivyo mpumbavu
asivyostahili heshima. 2 Kama shorowanda hurukaruka na kumeza wadudu wakati
wa kuruka, ndivyo ilivyo laana isiyostahili haishuki. 3 Mjeledi ni kwa ajili ya farasi,
hatamu kwa ajili ya punda na fimbo ni kwa ajili mgongo wa wapumbavu. 4 Usimjibu
mpumbavu na kujiunga katika upumbavu wake, au utakuwa kama yeye. 5 Mjibu
mpumbavu na jiunge katika upumbavu wake, ili asiweze kuwa na busara katika
macho yake mwenyewe. 6 Anayetuma ujumbe kwa mkono wa mpumbavu huikata
miguu yake mwenyewe na kunywa vurugu. 7 Miguu ya kiwete inayoning'ia chini ni
kama mithali kwenye kinywa cha wapumbavu. 8 Kujaribisha jiwe kwenye kombeo ni
sawa na kumpa heshima mpumbavu. 9 Mwiba unaochoma kwenye mkono wa mlevi
ni kama mithali kwenye kinywa cha wapumbavu. 10 Mpiga mishale anayejeruhi
kila mtu ni kama mtu anayemwajiri mpumbavu au kila mtu anayepita karibu yake.
11 Kama mbwa anavyorudia matapishi yake, ndivyo alivyo mpumbavu anayerudia
upuuzi wake. 12 Je unamwona mtu mwenye busara katika macho yake mwenyewe?
Mpumbavu anamatumaini zaidi kuliko yeye. 13 Mtu mvivu husema “ Kuna simba
kwenye barabara! Kuna simba katikati ya njia kuu!” 14 Kama mlango unavyogeuka
kwenye bawaba zake, ndivyo alivyo mtu mvivu kwenye kitanda chake. 15 Mtu mvivu
hutia mkono wake kwenye sufuria na bado hana nguvu kuunyanyua kwenda kwenye
kinywa chake. 16 Mtu mvivu ni mwenye hekima kwenye macho yake mwenyewe
kuliko watu saba wenye ufahamu. 17 Kama mtu anayeshikilia masikio ya mbwa,
ndivyo alivyo mpitajia anayepata hasira kwenye ugomvi ambao si wake. 18 Kama
mtu mwendawazimu anayetupa mishale, 19 ndivyo alivyo ambaye humdanganya
jirani yake na kusema, “ Je sikuwa naongea utani?” 20 Kwa kukosa kuni, moto
huzimika; na pale pasipo na mmbea ugomvi hukoma. 21 Mkaa ni kwa kuwasha
makaa na kuni kwa ajili ya moto, ndivyo alivyo mtu mgomvi kwa kuwasha ugomvi.
22 Maneno ya mmbea ni kama chembe tamu; nazo zinashuka chini kwenye sehemu
za ndani ya mwili. 23 Kioo kinachofunika chombo cha udongo ni kama midomo
inayoungua na moyo mbaya. 24 Yule ambaye huwachukia wengine huficha hisia
zake kwa midomo na hufunika uongo ndani yake mwenyewe. 25 Ataongea kwa
huruma, lakini usimwamini, maana kuna machukizo saba kwenye moyo wake.
26 Ingawa chuki zake zimefunikwa kwa udanganyifu, uovu wake utakuwa wazi katika
kusanyiko. 27 Anayechimba shimo atatumbukia ndani yake na jiwe litamsaga yule
anayelisukuma. 28 Ulimi wa uongo huchukia watu unaowajeruhi na kinywa cha
uongo husogeza karibu uharibifu.

# 27

1 Usijisifu kwa ajili ya kesho, maana hujui siku italeta nini. 2 Mtu mwingine akusifu
na wala si kinywa chako mwenyewe, mgeni na wala si midomo yako mwenyewe.
3 Fikiria uzito wa jiwe na uzito wa mchanga- uchokozi wa mpumbavu ni mzito zaidi
kuliko hivyo vyote. 4 Kuna ukatili wenye ghadhabu kali na mafuriko ya hasira, lakini
ni nani anayeweza kusimama mbele ya wivu? 5 Ni bora karipio la wazi kuliko
upendo uliofichwa. 6 Mwaminifu ni jeraha zilizosababishwa na rafiki, lakini adui
anaweza kukubusu kwa kuomba radhi mno. 7 Mtu aliyekula na kushiba hulikataa
hata sega la asali, bali kwa mtu mwenye njaa, kila kitu kichungu ni kitamu. 8 Ndege
anayezurura kutoka kwenye kiota chake ni kama mtu anayepotea sehemu ambayo
anaishi. 9 Pafumu na manukato huufanya moyo ufurahi, lakini utamu wa rafiki
ni bora kuliko ushauri wake. 10 Usimwache rafiki yako na rafiki wa baba yako,
na usiende kwenye nyumba ya ndugu yako katika siku ya msiba wako. Ni bora
rafiki ambaye yupo karibu kuliko ndugu ambaye yupo mbali. 11 Mwanangu, uwe na

busara, moyo wangu ufurahi; kisha nitamjibu yule anayenidhihaki. 12 Mtu mwenye
busara huiona taabu na kujificha mwenyewe, lakini mjinga huendelea mbele na
kuteseka kwa ajili ya taabu. 13 vazi kama mwenyewe anaweka pesa kama dhamana
kwa deni la mgeni; lichukue kama anaweka dhamana kwa malaya. 14 Anayempa
jirani yake baraka kwa sauti ya juu mapema asubuhi, baraka hiyo itafikiriwa kuwa
laana! 15 Mke mgomvi ni kama siku ya manyunyu ya mvua ya daima; 16 kumzuia
ni kama kuuzuia upepo, au kujaribu kushika mafuta kwa mkono wako wa kulia.
17 Chuma hunoa chuma; kwa njia ile ile; mtu humnoa rafiki yake. 18 Yule anayeutunza
mtini atakula matunda yake, na yule mwenye kumlinda bwana wake ataheshimiwa.
19 Kama maji yanavyoakisi taswira ya sura ya mtu, ndivyo hivyo moyo wa mtu
humwaksi mtu. 20 Kama kuzimu na Uharibifu havitosheki, ndivyo yalivyo macho ya
mtu hayawezi kutosheka. 21 Kalibu ni kwa fedha na tanuru ni kwa dhahabu; na mtu
hujaribiwa anaposifiwa. 22 Hata kama utamponda mpumbavu kwa mchI- pamoja
na nafaka- bado upumbavu wake hautatoka. 23 Hakikisha unajua hali ya makundi
yako na ujishughulishe juu ya makundi yako, 24 maana utajiri haudumu daima. Je taji
hudumu kwa vizazi vyote? 25 Majani huondoka na ukuaji mpya huonekana na milima
ya chakula cha mifugo hukusanywa ndani. 26 Wanakondoo watakupatia mavazi yako
na mbuzi watakupatia gharama ya shamba. 27 Kutakuwa na maziwa ya mbuzi kwa
chakula chako- chakula kwa kaya yako- na chakula kwa watumishi wako wasichana.

# 28

1 Waovu hukimbia wakati hakuna mtu anayewafukuza, bali wale watendao haki
ni thabiti kama simba kijana. 2 Kwa sababu ya uhalifu wa nchi, kuna wakuu wengi,
bali kwa mtu mwenye ufahamu na maarifa, itadumu kwa muda mrefu. 3 Mtu
masikini mwenye kukandamiza watu wengine masikini ni kama mvua inayopiga
ambayo haisazi chakula. 4 Wale wanaokataa sheria huwatukuza watu waovu, bali
wale wenye kuitunza sheria hupigana dhidi yao. 5 Watu wabaya hawafahamu haki,
bali wale wanaomtafuta Yehova wanafahamu kila kitu. 6 Ni bora mtu masikini
ambaye anatembea katika uadilifu, kuliko mtu tajiri ambaye ni mdanganyifu katika
njia zake. 7 Yeye anayetunza sheria ni mwana mwenye ufahamu, bali mwenye
ushirika na walafi humwaibisha baba yake. 8 Anayepata mafanikio kwa kutoza riba
kubwa anakusanya utajiri wake kwa ajili ya mwingine ambaye atakuwa na huruma
kwa watu masikini. 9 Kama mtu atageuzia mbali sikio lake kusikia sheria, hata
maombi yake ni chukizo. 10 Yeye anayempotosha mwenye uadilifu katika njia ya
uovu ataangukia kwenye shimo lake mwenyewe, bali wakamilifu watapata urithi
mwema. 11 Mtu tajiri anaweza kuwa mwenye hekima machoni pake mwenyewe,
bali mtu masikini mwenye ufahamu atamtafuta. 12 Kunapokuwa na ushindi kwa
wenye kutenda haki, kunafuraha kuu, bali wanapoinuka waovu, watu hujificha
wenyewe. 13 Yeye afichaye dhambi zake hatafanikiwa, bali mwenye kutubu na
kuziacha ataonyeshwa rehema. 14 Anafuraha ambaye huishi kwa unyenyekevu, bali
anayeufanya moyo wake ataanguka katika taabu. 15 Kama simba anayeunguruma
au dubu anayeshabulia ni kama mtawala mwovu juu ya watu masikini. 16 Mtawala
anayekosa ufahamu ni mkandamizaji katili, bali mwenye kuchukia aibu atadumu
katika siku zake. 17 Kama mtu anahatia kwa sababu amemwaga damu ya mtu,
atakuwa mkimbizi hadi kifo na hakuna atakayemsaidia. 18 Mwenye kuenenda kwa
ukaminifu atakuwa salama, bali mwenye njia ya udanganyifu ataanguka ghafla.
19 Anayefanya kazi kwenye shamba lake atapata chakula kingi, bali afuataye shughuli
za upuuzi atapata umasikini mkubwa. 20 Mtu mwaminifu atapata baraka nyingi bali
apataye utajiri wa haraka hawezi kukosa adhabu. 21 Siyo vema kuonyesha upendeleo,
lakini kwa kipande cha mkate mtu atafanya ubaya. 22 Mtu mchoyo huharakisha

kwenye utajiri, lakini hajui ni umasikini gani utakuja juu yake. 23 Anayemkaripia
mtu baadaye atapata fadhila zaidi kutoka kwake kuliko mwenye kumsifia sana kwa
ulimi wake. 24 Yule anayemwibia baba yake na mama yake na kusema, “ Hiyo
siyo dhambi,” ni mshirika wa mwenye kuharibu. 25 Mtu mwenye tamaa huchochea
mafarakano, bali anayemtumaini Yehova atafanikiwa. 26 Yule anayeutumaini moyo
wake mwenyewe ni mpumbavu, bali anayekwenda kwa hekima atajilinda mbali na
hatari. 27 Mwenye kuwapa masikini hatapungukiwa kitu, bali anayewafumbia macho
atapokea laana nyingi. 28 Watu waovu wanapoinuka, watu hujificha wenyewe, lakini
watu waovu wataangamia, wale watendao haki wataongezeka.

# 29

1 Mtu aliyepokea makaripio mengi lakini anashupaza shingo yake atavunjika ndani
ya muda mfupi na hata pona. 2 Watenda mema wanapoongezeka, watu wanafurahi,
bali wakati mtu mwovu anapotawala, watu huugua. 3 Mwenye kupenda hekima
baba yake anafurahi, bali anayeshikamana na makahaba huuharibu utajiri wake.
4 Mfalme huimarisha nchi kwa haki, bali mwenye kudai rushwa huirarua. 5 Mtu
anayejipendekeza kwa jirani yake anatandaza wavu kwenye miguu yake. 6 Mtu
mbaya hunaswa kwenye mtego wa dhambi yake mwenyewe, bali yeye atendaye
haki huimba na kufurahi. 7 Atendaye haki hutetea madai ya masikini; mtu mwovu
hafahamu maarifa kama hayo. 8 Mwenye dhihaka huutia moto mji, bali wale wenye
busara huigeuza ghadhabu. 9 Mtu mwenye busara anapojadiliana na mpumbavu,
hughadhabika na kucheka, hakutakuwa na utulivu. 10 Mkatili humchukia mwenye
ukamilifu na hutafuta maisha ya mwenye haki. 11 Mpumabavu huonyesha hasira
yake, bali mtu mwenye busara huishikilia na kujituliza mwenyewe. 12 Kama
matawala atazinagatia uongo, maafisa wake wote watakuwa waovu. 13 Mtu masikini
na mkandamizaji wanafanana, maana Yehova huyapa nuru macho yao wote. 14 Kama
mfalme atamhukumu masikini kwa uaminifu, kiti chake cha enzi kitaimarishwa
milele. 15 Fimbo na maonyo huleta hekima, bali mtoto huru mbali na makaripio
humwaibisha mama yake. 16 Watu waovu wanapotawala, uovu huongezeka, bali
wenye kutenda haki wataona anguko la watu waovu. 17 Mwadibishe mwanao naye
atakupa pumziko; ataleta furaha katika maisha yako. 18 Pasipo na maono ya kinabii
watu huenda bila utaratibu, bali mwenye kuitunza sheria amebarikiwa. 19 Mtumwa
hawezi kurekebishwa kwa maneno, maana ingawa anaelewa, hakuna mwitikio.
20 Je unamwona mtu mwenye haraka katika maneno yake? Kuna matumaini
zaidi kwa mpumbavu kuliko kwake. 21 Mwenye kumdekeza mtumwa wake tangu
ujana, mwisho wake itakuwa taabu. 22 Mtu mwenye hasira huchochea ugomvi na
bwana mwenye hasira sana hutenda dhambi nyingi. 23 Kiburi cha mtu humshusha
chini, bali mwenye roho ya unyenyekevu atapewa heshima. 24 Anayeshirikiana na
mwizi huyachukia maisha yake mwenyewe; husikia laana na wala hasemi chochote.
25 Kumwogopa binadamu ni mtego, bali mwenye kumtumaini Yehova atalindwa.
26 Wengi huutafuta uso wa mtawala, bali kutoka kwa Yehova huja haki kwa ajili
yake. 27 Mtu dhalimu ni chukizo kwa wenye kutenda haki, bali mwenye njia ya haki
ni chukizo kwa watu waovu.

# 30

1 Maneno ya Aguri mwana wa Yake - mausia: Mtu huyu alimwambia Ithieli,
kwa Ithiel na Ukali: 2 Hakika nipo kama mnyama kuliko mwanadamu na sina
ufahamu wa wanadamu. 3 Sijajifunza hekima, wala sina maarifa ya Mtakatifu.
4 Je ni nani amekwenda juu mbinguni na kurudi chini? Je ni nani aliyekusanya
upepo kwenye mikono yake? Je ni nani aliyekusanya maji kwenye kanzu? Je

ni nani aliyeziimarisha ncha za dunia yote? Jina lake ni nani, na jina la mtoto
wake ni nani? Hakika unajua! 5 Kila neno la Mungu limejaribiwa, yeye ni ngao
kwa wale wanaokimbilia kwake. 6 Usiyaongezee maneno haya, au atakukemea, na
utathibitishwa kuwa mwongo. 7 Vitu viwili ninakuomba, usivikatalie kwangu kabla
sijafa: 8 Majivuno na uongo viweke mbali nami. Usinipe umasikini wala utajiri, nipe
tu chakula ninachohitaji. 9 Maana nikipata vingi zaidi, nitakukana wewe na kusema,
“ Yehova ni nani?” Au kama nitakuwa masikini, nitaiba na kukufuru jina la Mungu
wangu. 10 Usimkashifu mtumwa mbele ya bwana wake, au atakulaani na utapata
hatia. 11 Kizazi ambacho kinachomlaa baba yao na hakimbariki mama yao, 12 kizazi
hicho ni safi katika macho yao wenyewe, lakini hawajaoshwa uchafu wao. 13 Hicho
ni kizazi- jinsi gani macho yao yanakiburi na kope zao zimeinuka juu! - 14 kuna kizazi
ambacho meno yao ni upanga, na mifupa ya taya zao ni visu, ili waweze kumrarua
masikini wamtoe duniani na mhitaji atoke miongoni mwa wanadamu. 15 Ruba
anamabinti wawili, “ Toa na Toa” wanalia. Kuna vitu vitatu ambavyo havitosheki,
vinne ambavyo havisememi, “Inatosha”: 16 Kuzimu, tumbo tasa, nchi yenye kiu kwa
maji, na moto usiosema, “Inatosha.” 17 Jicho ambalo linamdhihaki baba na kudharau
utii kwa mama, macho yake yatadonolewa na kunguru wa bondeni, na ataliwa
na tai. 18 Kuna vitu vitatu ambavyo vinanishangaza, vinne ambavyo sivifahamu:
19 njia ya tai angani; njia ya nyoka juu ya mwamba; njia ya meli kwenye moyo wa
bahari; na njia ya mtu pamoja mwanake kijana. 20 Hii ni njia ya mzinzi- anakula
na kufuta kinywa chake na kusema, “sijafanya ubaya wowote.” 21 Chini ya vitu
vitatu dunia hutetemeka na vinne haiwezi kuvivumilia: 22 mtumwa anapokuwa
mfalme; mpumbavu anaposhiba vyakula; 23 mwanamke anayechukiwa anapoolewa;
kijakazi anapochukua nafasi ya mkuu wake. 24 Vitu vinne duniani ni vidogo na bado
vinabusara: 25 mchwa ni viumbe ambao sio imara, lakini huandaa chakula chao
wakati wa hari, 26 Wibari siyo viumbe wenye nguvu, lakini hutengeneza makazi yake
kwenye miamba. 27 Nzige hawana mfalme, lakini wote wanamwendo wa mpangilio.
28 Kama mjusi, unaweza kumkunja kwa mikono yako miwili, lakini wanapatikana
katika majumba ya wafalme. 29 Kuna vitu vitatu ambavyo ni fahari katika mwendo na
vinne ambavyo ni fahari katika namna ya kutembea: 30 simba, aliyeimara miongoni
mwa wanyama- wala hajiepushi na kitu chochote; 31 jogoo anayetembea kwa mikogo;
mbuzi; na mfalme ambaye askari wapo kando yake. 32 Kama umekuwa mpumbavu,
jitukuze mwenyewe, au kama umekuwa ukisimamia vibaya- weka mkono wako juu
ya kinywa chako. 33 Kama kusuka maziwa hufanya siagi na pua ya mtu hutoa damu
kama imepigwa, basi matendo yanayofanywa kwa hasira huzalisha mafarakano.

# 31

1 Maneno ya mfalme Lemueli - mausia aliyofundishwa na mama yake. 2 Mwanangu
nini? Na ni nini mwana wa tumbo langu? Na ni nini mwana wa nadhiri zangu?
3 Nguvu zako usiwape wanawake; au wenye kuharibu wafalme njia zako. 4 Lemueli,
kunywa divai, siyo kwa ajili ya wafalme, wala kwa watawala kuuliza, “ kileo
kikali kiko wapi?” 5 Kwa sababu kama watakunywa, watasahau sheria ni nini, na
kupotosha haki za wote walioonewa. 6 Wape kileo kikali watu wanaopotea na mvinyo
kwa wale wenye kutaabika kwa uchungu. 7 Atakunywa na kusahau umasikini
wake na hataikumbuka taabu yake. 8 Ongea kwa ajili yao wasioweza kuongea,
kwa madai ya wote wanaopotea. 9 Ongea na uhukumu kwa vipimo vya haki na
utetee dai la masikini na watu wahitaji. 10 Mke hodari ni nani anaweza kumpata?
Thamani yake ni zaidi kuliko vito. 11 Moyo wa mume wake humwamini, na hatakuwa
masikini. 12 Humtendea mambo mema na wala si mabaya siku zote za maisha yake.
13 Huchagua sufu na kitani, na hufanya kazi yake ya mikono kwa furaha. 14 Yupo

kama meli za wafanyabiashara; huleta chakula chake kutoka mbali. 15 Huamka
wakati wa usiku na kuwapa chakula watu wa kaya yake, na kugawa kazi kwa
watumishi wake wa kike. 16 Hulifikiria shamba na kulinunua, kwa tunda la mikono
yake hupanda shamba la mizabibu. 17 Yeye mwenyewe hujivika nguvu na kuimarisha
mikono yake. 18 Huangalia ni kipi kitaleta faida nzuri kwake; usiku wote taa yake
haizimishwi. 19 Mikono yake huiweka kwenye mpini wa kisokotea nyuzi na hushikilia
kisokotea nyuzi. 20 Mkono wake huwafikia watu masikini; mikono yake huwafikia
watu wahitaji. 21 Haogopi theluji kwa ajili ya kaya yake, kwa maana nyumba yake
yote imevika kwa nguo nyekundu. 22 Hutengeneza matandiko ya kitanda chake, na
huvaa nguo za kitani ya dhambarau safi. 23 Mume wake anajulikana malangoni,
anapoketi na wazee wa nchi. 24 Hutengeneza mavazi ya kitani na kuyauza, na
naleta mishipi kwa wafanyabiashara. 25 Amevaa nguvu na heshima, na wakati
ujao huucheka. 26 Anafumbua kinywa chake kwa hekima na sheria ya ukarimu ipo
kwenye ulimi wake. 27 Huangalia njia za nyumba yake na hawezi kula mkate wa
uvivu. 28 Watoto wake huinuka na kumwita heri na mume wake humsifia, akisema,
29 “Wanawake wengi wamefanya vizuri, lakini wewe umewapita wote.” 30 Madaha ni
udanganyifu, uzuri ni ubatili; bali mwanamke amchaye Yehova, atasifiwa. 31 Mpeni
tunda la mikono yake na kazi zake zimsifu katika malango.

# Mhubiri

1 Haya ni maneno ya Mwalimu, mwana wa Daudi na mfalme katika Yerusalemu.
2 Mwalimu asema hivi, “Kama mvuke wa ukungu, kama upepo mwanana katika
upepo, kila kitu hutoweka na kuacha maswali mengi. 3 Ni faida gani wanadamu
huipata kutoka katika kazi zote wazifanyazo chini ya jua? 4 Kizazi kimoja huenda,
na kizazi kingine huja, lakini nchi yabaki milele. 5 Jua huchomoza na jua huzama na
kwenda kwa kasi, na kurudi mahali linapochomozea tena. 6 Upepo huvuma kusini na
huzunguka kasikazi, na mara zote ukizunguka katika njia yake na kurudi tena. 7 Mito
yote hutiririka katika bahari, lakini bahari haijai. Mahali mito inakoenda, ndiko
inakoenda tena. 8 Kila kitu huwa uchovu, na hakuna yeyote awezae kukielezea. Jicho
halishibina kile linachokiona, wala sikio halishibi na kile linachosikia. 9 Chochote
kilichopo ndicho kitakachokuwepo, kila kilichofanyika ndicho kitakachofanyika.
Hakuna jipya chini ya jua. 10 Je kuna jambo lolote ambalo watu wanaweza kusema,
'Tazama, hili ni jipya'? Chochote kilichopo kimekwisha kuwepo muda mwingi, wakati
uliokuwepo kabla yetu. 11 Hakuna anayeonekana kukumbuka kilichotokea nyakati
za zamani. Na mambo yaliyo tokea siku zilizo pita na yale yatakayo tokea siku za
mbele nayo hayatakumbukwa.” 12 Mimi ni mwalimu, na nimekuwa mfalme juu
ya Isareli katika Yerusalemu. 13 Nilitia akili yangu katika kusoma na kutafuta kwa
hekima kila kitu kinachofanywa chini ya mbingu. Hili nalo ni jukumu zito ambalo
Mungu amewapa wana wa watu kujishughulisha nalo. 14 Nimeona matendo yote
ambayo yanafanyika chini ya jua, na tazama yote ni mvuke ni kujaribu kuuchunga
upepo. 15 Palipopinda hapawezi kunyoshwa! Kisicho kuwepo hakiwezi kuhesabiwa!
16 Nimeuambia moyo wangu nikisema, “Tazama, nimepata hekima kubwa kuliko
walioishi Yerusalemu kabla yangu. Akili yangu imeona hekima kubwa na ufahamu.”
17 nimetia moyo wangu kujua hekima na upumbuvu na ujinga. Nikagundua kuwa
hili nalo pia lilikuwa ni kujaribu kuuchunga upepo. 18 Kwa kuwa katika wingi wa
hekima kuna masumbufu mengi, naye aongezae ujuzi, aongeza masikitiko.

## 2

1 Nikasema moyoni, “Njoo, na nitakujaribu kwa kwa furaha. Kwa hiyo furahia.”
Lakini tazama, huu nao ulikuwa ni upepo wa muda. 2 Nikasema juu ya kicheko,
“Ni wazimu,” na kuhusu furaha, “Yafaa nini?” 3 Nikajipeleleza moyoni mwangu
katika jinsi ya kutimiza hamu yangu kwa mvinyo. Nikaruhusu akili yangu iongozwe
na hekima ingawa bado nilikuwa nikishikilia ujinga. Nilitaka kutafuta jambo lililo
jema kwa wanadamu kufanya chini ya mbingu wakati wa siku za maisha yao.
4 Nilitimiza mambo makubwa. Nilijenga nyumba kwa ajili yangu na kupanda miti
ya mizabibu. 5 Nilitengeneza bustani na viwanja; nikapanda aina zote za matunda
ndani yake. 6 Nikatengeneza mabwawa ya maji ili kumwagilia msitu mahali miti
ilikuwa imepandwa. 7 Nilinunua watumwa wa kiume na wa kiume; nilikuwa na
watumwa waliozaliwa katika ikulu yangu. Pia nikawa na makundi makubwa na
wanyama wa kufugwa, zaidi ya mfalme yeyote aliyetawala kabla yangu katika
Yerusalemu. 8 Pia nilijikusanyia fedha na dhahabu, hazina ya wafalme na majimbo.
Nikapata waimbaji wanaume na wanawake kwa ajili yangu, na kufurahia kutoka kwa
wana wa wanadamu, masulia na wanawake. 9 Hivyo nikawa mkuu na tajiri kuliko
wote waliokuwa Yerusalemu kabla yangu, na hekima yangu ilikuwa ndani yangu.
10 Lolote ambalo macho yangu yalikitamani sikuyazuia. Sikuuzuia moyo wangu
katika furaha yeyote, kwa sababu moyo wangu ulifurahi katika katka kazi yangu

zote na furaha ilikuwa ni tunu kwa kazi zangu zote. [11] Kisha nikatazama matendo
yote ambayo mikono yangu iliyokwisha kuyatimiliza na juu ya kazi niliyokuwa
nimeifanya, lakini tena, kila kitu kilikuwa ni mvuke na kujaribu kuuchunga upepo.
Hakukuwa na faida chini ya jua. [12] Kisha nikageuka kuipambanua hekima, na
upumbavu na ujinga. Kwa maana ni kitu gani mfalme anayekuja baada yangu afanye,
ambacho hakijafanyika? [13] Kisha nikaanza kuelewa kwamba hekima ina faida kuliko
upumbavu, kama nuru ilivyo bora kuliko giza. [14] Mwenye hekima hutumia macho
yake katika kichwa chake kuona mahali anakoenda, lakini mpumbavu hutembea
katika giza, ingawa ninafahamu kuwa mwisho wa aina moja umetunzwa kwa kila
mmoja. [15] Kisha nikasema moyoni mwangu, “Kinachotokea kwa mpumbavu, ndicho
kitachotokea na kwangu. Hivyo kuna utofauti gani kama mimi ni mwenye hekima
sana?” Nikahitimisha moyoni mwangu, “Huu pia ni mvuke tu.” [16] Kwa kuwa mwenye
hekima, kama mpumbavu, hakumbukwi kwa muda mrefu. Katika siku zijazo, kila
kitu kitakuwa kimesahauliwa. Mwenye hekima hufa kama navyokufa mpumbavu.
[17] Hivyo nikauchukia uhai kwa sababu kazi zote zilizofanyika chini ya jua zilikuwa
mbaya kwangu. Hii ni kwa sababu kila kitu ni mvuke na kujaribu kuuchunga upepo.
[18] Nikachukia yote niliyoyatimiza, ambayo nilikuwa nimekwisha yafanya chini ya
jua kwa sababu ni lazima niyaache kwa mtu anaye kuja baada yangu. [19] Na ni nani
ajuaye kama atakuwa mwenye hekima au mpumbavu? Ila atakuwa msimamizi juu
ya kila kitu chini ya jua ambayo kazi yangu na hekima yangu imeyajenga. Huu
pia ni mvuke. [20] Kwa hiyo moyo wangu ukaanza kukata tamaa juu ya kazi zote
nilizozifanya chini ya jua. [21] Kwa kuwa kunaweza kuwa na mtu anayefanya kazi kwa
hekima, ufahamu, na umahili, lakini ataacha kila kitu alichonacho kwa mtu ambaye
hajafanya chochote. Huu nao ni mvuke na hatari kubwa. [22] Kwa maana ni faida gani
mtu hupata ambaye hufanya kazi kwa juhudi na kujaribu moyoni mwake kutimiza
kazi zake chini ya jua? [23] Kila siku kazi yake ni maumivu na masikitiko, hivyo wakati
wa usiku roho yake haipumziki. Huu pia ni mvuke. [24] Hakuna jambo jema kwa
mtu yeyote zaidi ya kula na kunywa na kuridhika na kile kilichochema katika kazi
yake. Nikaona kwamba ukweli huu unatoka kutoka mkononi mwa Mungu. [25] Kwa
kuwa ni nani anaweza kula au anaweza kupata furaha yoyote tofauti na Mungu?
[26] Kwa kuwa kwa kila anayemfurahisha yeye, Mungu humpa hekimana ufahamu
ba furaha. Ingawa, kwa mwenye dhambi humpa kazi ya kukusanya na kutunza ili
kwamba ampe mtu anayempendeza Mungu. Huu pia ni sawa na mvuke na kujaribu
kuuchunga upepo.

# 3

[1] Kwa kuwa kila kitu na wakati wake, na majira kwa kila kusudi chini ya mbingu.
[2] Kuna wakati wa kuzaliwa na wakati wa kufa, wakati wa kupanda na wakati wa
kung'oa yaliyopandwa, [3] wakati wa kuua na wakati wa kuponya, wakati wa kubomo
na wakati wa kujenga. [4] Kuna wakati wa kulia na wakati wa kucheka, wakati wa
kuomboleza na wakati kucheza, [5] wakati wa kutupa mawe na wakati wa kukusanya
mawe, wakati wa kukumbatia watu wengine wakati wa kutokumbatia. [6] Kuna wakati
wa kutafuta vitu na wakati wa kutotafuta, wakati wa kutunza vitu na wakati wa
kuvitupa, [7] wakati kuchana mavazi na wakati wa kuyashona, wakati wa kunyamaza
na wakati wa kuzungumza. [8] Kuna wakati wa kupenda na wakati wa kuchukia,
wakati wa vita na wakati wa amani. [9] Ni faida gani mfanyakazi aipatayo katika kazi
yake? [10] Nimeona kazi ambayo Mungu amewapa wanadamu kuitimiza. [11] Mungu
amefanya kila kitu kufaa kwa wakati wake. Pia ameweka umilele ndani ya mioyo
yao. Lakini mwanadamu hawezi kuelewa matendo ambayo Mungu ameyafanya,
tangu mwanzo wao hadi mwisho. [12] Ninajua kuwa hakuna kilicho bora kwa mtu

yeyote kuliko kufurahi na kutenda mema maadamu anaishi- 13 na kwamba kila
mmoja anapaswa ale na kunywa na anapaswa kuelewa jinsi ya kufurahia mazuri
ambayo yanatoka katika kazi zake zote. Hii ni zawadi kutoka kwa Mungu. 14 Ninajua
kwamba chochote afanyacho Mungu kinadumu milele. Hakuna kinaweza kuongezwa
au kuondolea, kwa sababu Mungu ndiye aliyekifanya, ili kwamba watu wamsogelee
kwa heshima. 15 Chochote kilichopo kimekwisha kuwepo; chochote kitakachokuwepo
kimekwisha kuwepo. Mungu huwafanya wanadamu kutafuka vitu vilivyjificha. 16 Na
nimeona kwamba chini ya jua ubaya upo mahali palipopaswa kuwa na haki, na
sehemu ya haki mara nyingi ina ubaya. 17 Nikasema moyoni mwangu, “Mungu
atahukumu mwenye haki na mbaya kwa wakati muafaka kwa kila jambo na kila
tendo. 18 Nikasema moyoni mwangu, “Mungu huwajaribu wanadamu kuwaonyesha
kwamba wao ni kama wanyama.” 19 Kwa kuwa mwisho watoto wa wanadamu na
mwisho wa wanyama ni sawa. Kifo cha mmoja ni sawa na kifo cha mwingine. Wote
wana pumzi sawa. Hakuna faida kwa mwanadamu zaidi ya wanyama. Kwa kuwa
hakuna kila kitu isipokuwa pumzi? 20 Kila kitu kinaenda sehemu moja. Kila kitu
kinatoka mavumbini, na kila kitu kinarudi katika mavumbini. 21 Ni nani ajuaye kama
roho ya mwanadamu inaenda juu na roho ya wanyama inaenda chini ya nchi? 22 kwa
hiyo tena nikatambua kwamba hakuna lililo jema kwa yeyote zaidi ya kufurahia
kazi yake, kwa kuwa hilo ndilo jukumu lake. Ni nani awezaye kumleta tena kuona
kinachotokea baada yake?

# 4

1 Kisha tena nikafikiri kuhusu mateso yote yaliyo chini ya jua. Tazama machozi ya
watu walioteswa. Hakuna anaye mfariji kwa ajili yao. Nguvu iko katika mikononi
mwa watesaji, lakini wateswaji hawana mfariji. 2 Hivyo nikawapongeza watu walio
kufa, wale ambao tayari wamekufa, sio wanaoishi, wale ambao wako hai. 3 Ingawa,
bahati zaidi kuliko wote wawili ni yule ambaye hajaishi, yeye ambaye hajaona
matendo yoyote mabaya ambayo yanafanyika chini ya jua. 4 Kisha nikaona kwamba
kila tendo la kazi na kila kazi ya utashi ikawa wivu wa jirani ya mtu. Huu pia ni
mvuke na kujaribu kuchunga upepo. 5 Mpumbavu hukunja mikono yake na hafanyi
kazi, hivyo chakula chake in mwili wake. 6 Lakini afadhari konzi ya faida pamoja
na kazi ya haraka kuliko konzi mbili pamoja na kazi ambayo hujaribu kuuchunga
upepo. 7 Kisha nikafikiri tena zaidi kuhusu ubatili, mvuke upoteao zaidi chini ya jua.
8 Kuna aina ya mtu ambaye yuko peke yake. Hana mtu, hana mwana, wala ndugu.
Hakuna mwisho wa kazi zake zote, na macho yake hayatosheki kwa kupata utajiri.
Anashangaa, “Ninajishumbua na kuharibu furaha yangu kwa ajili ya nani?” Huu pia
ni mvuke, hali mbaya. 9 Watu wawili wanafanya vizuri zaidi ya mmoja; kwa pamoja
wanaweza kupata malipo mazuri kwa ajili ya kazi yao. 10 Kwa kuwa kama mmoja
akianguka, mwingine anaweza kumwinua rafiki yake. Ingawa, huzuni humfuata
yeye aliye peke yake anapoanguka kama hakuna mtu wa kumwinua. 11 Na kama
wawili wakilala pamoja, wanaweza kupata joto, lakini mtu mmoja anawezaje kupata
joto akiwa mwenyewe? 12 Mtu akiwa peke yake anaweza kushindwa nguvu, lakini
wawili wanaweza kusimama katika shambulio, na kama ya nyuzi tatu haikatika
upesi. 13 Ni bora kuwa kijana masikini kuliko kuwa mfalme mzee na mpumbavu
ambaye hajui jinsi ya kusikiliza maonyo. 14 Hii ni kweli hata kama mtu mdogo
anapokuwa mfalme kutoka gerezani, au hata kama alizaliwa masikini katika ufalme
wake. 15 Ingawa, niliona kila mmoja aliye kuwa hai na kuzunguka chini ya jua
wakijitia chini kwa kijana mdogo aliyeinuka kama mfalme. 16 Hakuna mwisho kwa
watu wote wanaotaka kumtii mfalme mpya, lakini wengi wao hawatamsifu yeye.
Hakika hali hii ni mvuke na kujaribu kuuchunga upepo.

# 5

[1] Linda mwenendo wako unapoenda kwenye nyumba ya Mungu. Nenda kule
usikilize. Kusikiliza ni bora kuliko wapumbavu wanapotoa dhabihu wakati hawa-
juikuwa wanachofanya katika maisha ni kibaya. [2] Usiwe mwepesi wa kuongea kwa
mdomo wako, na usiufanye moyo wako kuleta jambo lolote kwa haraka mbele za
Mungu. Mungu yuko mbinguni, lakini uko chini, kwa hiyo maneno yako yawe
machache. [3] Kama una mambo mengi ya kufanya na kuhangaika, pengine utapata
ndoto mbaya. Na pengine utaongea maneno mengi ya upumbavu. [4] Ukiweka nadhili
kwa Mungu, usichelewe kuifanya, kwa kuwa Mungu hafurahii upumbavu. Fanya kile
ulichoapa utakifanya. [5] Ni bora kutokuweka nadhiri kuliko kuweka nadhiri ambayo
usiyoiondoa. [6] Usiuruhusu mdomo wako kusababisha mwili wako kutenda dhambi.
Usiseme kwa mtumwa wa kuhani, "Kile kiapo kilikuwa kwa makosa." Kwani nini
kumfanya Mungu akasirike kwa kuapa kwa uongo, kumchochea Mungu aharibu
kazi ya mikono yako? [7] Kwa kuwa katika ndoto nyingi, kama ilivyo katika maneno
mengi, kuna mvuke ubatili. Hivyo mwogope Mungu. [8] Unapomwona masikini
akiteswa na kunyang'anywa haki na kutendewa vibaya katika jimbo lako, usishangae
kama kwamba hakuna anaye fahamu, kwa sababu kuna watu katika mamlaka
ambao hutazama, kuna hata walio juu yao. [9] Kwa nyongeza uzalishaji wa ardhi
ni kwa kila mmoja, na mfalme mwenyewe huchukua uzalishaji kutoka mashambani.
[10] Yeyote apendaye fedha hatatosheka na fedha, na yeyote apendaye utajiri mara
zote hutaka zaidi. Huu pia ni mvuke. [11] Kadri mafanikio yanapoongezeka, ndivyo
wanavyoongezeka watu wanaotumia. Kuna faida gani katika utajiri kwa mmiliki
isipokuwa kuutazama kwa macho yake? [12] Usingizi wa mfanyakazi ni mtamu, kama
anakula kidogo au sana, lakini utajiri wa mtu tajiri haumuruhusu yeye kulala vizuri.
[13] Kuna jambo baya zaidi ambalo nimeliona chini ya jua: mali iliyowekwa akiba na
mwenye nayo, inamsababishia taabu mwenyewe. [14] Wakati tajiri anapopoteza utajiri
wake kwa bahati mbaya, mwana wake, ambaye amemzaa, habakiziwi chochote
mikononi mwake. [15] Kama mtu azaliwavyo uchi kutoka tumboni mwa mamaye,
vivyo hivyo ataondoka katika maisha haya akiwa uchi. Hachukui chochote kutoka
katika kazi yake. [16] Jambo jingine baya kabisa, kama mtu alivyo kuja ni lazima
aende vivyo hivyo. Hivyo ni faida gani mtu yeyote aipatayo katika kufanya kwa
ajili ya upepo? [17] Wakati wa siku zake anakula gizani na anafedheheshwa sana
na magonjwa na hasira. [18] Tazama, kile nilichokiona kuwa kizuri kufaaa ni kula
na knywa na kufurahia faida kutoka katika kazi zetu zote, tuzifanyazo chini ya jua
wakati wa siku za maisha haya ambayo Mungu ametupa. Kwa kuwa huu ni wajibu
wa mtu. [19] Yeyote ambaye Mungu amempa mali na utajiri na uwezo wa kupokea
sehemu yake na kufurahi katika kazi yake hii ni zawadi kutoka kwa Mungu. [20] Kwa
kuwa mara kadhaa hakumbuki siku za maisha yake, kwa sababu Mungu anamfanya
kuhangaika na mambo ambayo anafurahia kuyafanya.

# 6

[1] Kuna ubaya ambao nimeuona chini ya jua, na ni mbaya kwa watu. [2] Mungu
anaweza kumpa mtu mali na utajiri na heshima kwa kiasi kwamba hakosi chochote
anachokitamani mwenyewe, lakini kisha hampi uwezo wa kukifurahia. Badala
yake mtu mwingine hutumia vitu vyake. Huu ni mvuke, teso baya. [3] Kama
mtu akizaa watoto mia moja na kuishi miaka mingi, ili kwamba siku za miaka
yake ni nyingi, lakini kama moyo wake hautosheki kwa mema na hazikwi kwa
heshima, kisha ninasema kwamba, mtoto aliyezaliwa akiwa amekufa ni bora kuliko
alivyo. [4] Hata mtoto huyo amezaliwa bila faida na anapita katika giza, na jina
lake linabaki limefichika. [5] Ingawa mtoto huyu haoni jua au kujua kitu chochote,

ana pumziko ingawa mtu huyo hakupumzika. [6] Hata kama mtu akiishi miaka
elfu mbili lakini hajifunzi kufuraia vitu vizuri, aenda sehemu moja kama mtu
yeyote yule. [7] Ingawa kazi yote ya mtu ni kujaza mdomo wake, ila hamu yake
haishibi. [8] Hakika ni faida gani aliyo nayo mwenye hekima kuliko mpumbavu?
Ni faida gani aliyo nayo masikini hata kama anajua jinsi ya kutenda mbele ya
watu? [9] Ni bora kuridhika na kile ambacho macho hukiona kuliko kutamani kile
ambacho hamu isiyo tulia inatamani, ambayo pia ni mvuke na kujaribu kuuchunga
upepo. [10] Chochote ambacho kimekuwepo, tayari kimekwisha kupewa jina lake,
na vile mtu alivyo ni kama tayari amekwisha fahamika. Hivyo imekuwa haifai
kugombana na yule ambaye ni muhukumu mkuu wa wote. [11] Maneno mengi ambayo
yanaongelewa, ndivyo yasiyo na maana yanaongezeka, kwa hiyo ni faida gani iliyopo
kwa mwanadamu? [12] Kwa kuwa ni nani ajuaye nini kilicho kizuri kwa mtu katika
maisha yake wakati wa ubatili wake, siku zilizo hesabika ambazo kwa hizo anapita
kama kivuri? Ni nina anayeweza kumwambia mtu kile kitakacho kuja chini ya jua
baada ya kupita?

# 7

[1] Jina zuri ni bora kuliko manukato ya gharama, na siku ya kufa ni bora kuliko siku
ya kuzaliwa. [2] Ni bora kwenda kwenye nyumba ya maombolezo kuliko nyumba ya
karamu, kwa kuwa maombolezo huja kwa watu wote wakati wa mwisho wa uhai,
kwa hiyo watu wanaoishi ni lazima waweke hili moyoni. [3] Huzuni ni bora kuliko
kicheko, kwa kuwa baada ya uso wa huzuni huja furaha ya moyo. [4] Moyo wa mwenye
hekima uko katika nyumba ya maombolezo, lakini moyo wa wapumbavu uko katika
nyumba ya karamu. [5] Ni bora kusikiliza maonyo ya mtu mwenye hekima kuliko
kusikiliza wimbo wa wapumbavu. [6] Kwa kuwa kama mlio wa miiba chini ya chungu,
ndivyo kilivyo kicheko cha wapumbavu. Huu pia ni mvuke. [7] kweli jeuri humfanya
mtu mwenye hekima kuwa mpumbavu, na rusha huharibu moyo. [8] Ni heri mwisho
wa jambo kuliko mwanzo; na watu wenye uvumilivu ni bora kuliko wenye majivuno
rohoni. [9] Usikasirike haraka rohoni mwako, kwa sababu hasira hukaa katika mioyo
ya wapumbavu. [10] Usiseme, “Kwa nini siku za zamani zilikuwa bora kuliko siku hizi?”
Kwa kuwa sio kwa sababu ya hekima kwamba unauliza swali hili. [11] Hekima ni njema
kama vitu vya thamani tunavyorithi kutoka kwa wazazi wetu. Inatoa faida kwa
wale wanaoliona jua. [12] Kwa kuwa hekima hutoa ulinzi kama vile fedha inavyoweza
kutoa ulinzi, lakini faida ya maarifa ni kwamba hekima humpa uhai kwa yeyote
aliye nayo. [13] Tafakaria matendo ya Mungu: Ni nani awezaye kuimarisha chochote
alichokipindisha? [14] Wakati nyakati vinakuwa njema, ishi kwa furaha katika hali
hiyo, lakini wakati unapokuwa mbaya, tafakari hili: Mungu ameruhusu hali zote
ziwepo, Kwa sababu hii, hakuna mwanadamu yeyote atakaye fahamu chochote
kinacho kuja baada yake. [15] Nimeona mambo mengi katika siku zangu za ubatili.
Kuna watu wenye haki ambao wanaangamia licha ya kwamba wana haki, na kuna
watu waovu wanaoishi maisha marefu licha ya kwamba ni waovu. [16] Usiwe mwenye
haki katika macho yako mwenyewe. Kwa nini kujiharibu mwenyewe? [17] Usiwe
mwovu sana au mpumbavu. Kwa nini ufe kabla ya wakati wako? [18] Ni vyema
kwamba ushike hekima hii, na kwamba usiache haki iende zake. Kwa kuwa mtu
amchae Mungu atatimiza ahadi zake zote. [19] Hekima ina nguvu ndani ya mwenye
hekima, zaidi ya watawala kumi katika mji. [20] Hakuna mtu mwenye haki juu ya
nchi anayefanya mema na hatendi dhambi. [21] Usisikilize kila neno linaongelewa,
kwa sababu unaweza kusikia mtumishi wako anakulaani. [22] Vivyo hivyo unafahamu
mwenyewe ndani ya moyo wako umewalaani wengine mara kadhaa. [23] Haya yote
nimeyathibitisha kwa hekima. Nikasema, “nitakuwa mwenye hekima,” lakini zaidi

ambavyo ningekuwa. 24 Hekima i mbali na kina sana. Ni nani awezaye kuipata?
25 Nikageuza moyo wangu kujifunza kuchunguza na kutafuta hekima na ufafanuzi
wa ukweli, na kufahamu kwamba ubaya ni ujinga na kwamba upumbavu ni wazimu.
26 Nikapata kufahamu kwamba uchungu kuliko kifo, ndivo alivyo mwanamke yeyote
ambaye moyo wake umejaa mitego, na nyavu, na ambaye mikono yake ni minyororo.
Yeyote ampendezaye Mungu ataponyoka kutoka kwake, lakini mwenye dhambi
atachukuliwa naye. 27 “Tafakari kile nilichovumbua,” asema Mwalimu. “Nimekuwa
nikiongeza uvumbuzi mmoja hadi mwingine ili kwamba nipate ufafanuzi wa ukweli.
28 Hii ndiyo bado natafuta, lakini bado sijapata. Sikupata mwanamme mmoja
mwenye haki miongoni mwa elfu, lakini sikupata mwanamke miongoni mwa wale
wote. 29 Nimegundua hili: kwamba Mungu alimuumba binadamu akiwa mnyoofu,
lakini wametoka katika hali ya unyofu wakitafuta magumu mengi.

# 8

1 Ni mtu gani mwenye hekima? Ambaye anafahamu matukio yana maana gani
katika maisha? Hekima ndani ya mtu husababisha uso wake kung'ara, na ugumu
wa uso wake hubadilika. 2 Ninakushauri kuitii amri ya mfalme kwa sababu ya kiapo
cha Mungu cha kumlinda yeye. 3 Usiharakishe kuondoka mbele ya uwepo wake,
na usisimame kuunga mkono jambo lisilofaa, kwa kuwa mfalme anafanya chochote
anacho tamani. 4 Neno la mfalme hutawala, kwa hiyo ni nani atakaye mwambia,
'Unafanya nini? 5 Yeyote ashikaye amri za mfalme hukwepa madhara. Moyo wa
mwenye hekima hutambua mwelekeo muafaka na muda wa kuenda. 6 Kwa kuwa
kila jambo lina jibu sahihi, na wakati wa kujibu, kwa sababu taabu ya mtu ni kubwa.
7 Hakuna anaye fahamu kinacho fuata. Ni nani awezaye kumwambia nini kinacho
kuja? 8 Hakuna mwenye uwezo juu ya roho aizuie roho; wala hana mamlaka juu
ya siku ya kufa; wala hakuna kuruhusiwa katika vita vile; wala uovu hautamwokoa
yule aliyeuzoea. 9 Mambo hayo yote nimeyaona, nikatia moyo wangu katika kila
kazi iliyofanyika chini ya jua. Kuna wakati ambapo mtu mmoja anayo mamlaka juu
ya mwenziwe kwa hasira yake. 10 Hivyo niliwaona wabaya wakizikwa hadharani.
Waliondolewa mahali patakatifu na kuzikwa mahali waliposifiwa na watu katika
mji walipokuwa wamefanya matendo maovu. Hii nayo haifai. 11 Wakati hukumu
dhidi ya tendo ovu haihukumiwi haraka, hushawishi mioyo ya wanadamu kutenda
ubaya. 12 Hata kama mwenye dhambi afanye uovu mara mia moja na bado aishi
kwa muda mrefu, bado ninafahamu itakuwa vyema kwa wale wanao muheshimu
Mungu, wanaouheshimu uwepo wake walio nao. 13 Lakini haitakuwa vyema kwa
mtu mwovu; mkewe hatacheleweshwa. Siku zake kama kizuri kitowekacho upesi,
kwa sababu hamuheshimu Mungu. 14 Kuna mvuke mwingine usio faa, jambo jingine
linaofanyika juu ya dunia. Mambo hutokea kwa watu wenye haki kama yatokeavyo
kwa watu waovu, na mambo hutokea kwa wenye haki kama yatokeavyo kwa waovu.
Ninasema hili pia ni mvuke usiofaa. 15 Kwa hiyo nikapendekeza furaha, kwa sababu
mtu hana jambo bora chini ya jua zaidi ya kula na kunywa na kuwa na furaha.
furaha ndiyo itamfuata katika kazi zake kwa siku zote za maisha yake ambayo Mungu
amempa chini ya jua. 16 Nikauweka moyo wangu kufamu hekima na kufahamu
kazi inayofanyika juu ya nchi, kazi ambayo inafanyika mara nyingi pasipo kufumba
macho usiku au mchana. 17 Kisha nika tafakari matendo yote ya Mungu, na kwamba
mtu hawezi kuelewa kazi inayofanyika chini ya jua. Bila kujali mtu anafanya kupata
majibu, hatayapata. Ingawa mwenye hekima anaweza kuamini anajua, kitu kweli
hajui.

# 9

1 Kwa kuwa nilifikiri haya yote katika akili zangu kufahamu kuhusu watu wenye
haki na wenye hekima na matendo yao. Wote wako katika mikono ya Mungu.
Hakuna anayefahamu kama upendo au chuki itakuja kwa mtu. 2 kila mmoja ana
mwisho sawa. Mwisho sawa una subiria watu wenye haki na waovu, wema,
walio safi na wasio safi, yeye atoaye dhabibu na yule asiye dhabihu. Kama vile
watu wema watakufa wenye dhambi nao watakufa vivyo hivyo. kama vile yule
anayeapa atakavyo kufa, vivyo hivyo mtu yule aogopaye kuweka kiapo naye atakufa.
3 Kuna mwisho mwovu kwa kila kitu kinachofanyika chini ya jua, na mwisho kwa
kila mtu. Moyo wa mwanadamu umejaa uovu, na wazimu uko katika mioyo yao
wakati wanaishi. Hivyo baada ya hilo wanaenda kwa wafu. 4 Kwa kuwa yeyote
anayeungana na wote walio hai kuna tumaini, kama vile mbwa aliye hai ni bora
kuliko simba aliye kufa. 5 Kwa kuwa watu walio hai, lakini walio kufa hawajui
chochote. Hawana tena tuzo yeyote kwa sababu kumbukumbu yao imesahaulika.
6 Upendo wao, chuki na wivu vimekatiliwa mbali muda mwingi. Hawatapata sehemu
katika kitu chochote kinachofanyika chini ya jua. 7 Nenda zako, kula mkate wako kwa
furaha, na kunywa mvinyo wako na moyo wa furaha, kwa kuwa Mungu huruhusu
kusherehekea kazi njema. 8 Nguo zako ziwe nyeupe siku zote, na kichwa chako
kipake mafuta. 9 Ishi kwa furaha na mwanamke umpendaye siku zako zote za maisha
yako ya ubatili, siku ambazo Mungu amekupatia chini ya jua wakati wa siku zako za
ubatili. Hiyo ni thawabu kwa ajili ya kazi yako chini ya jua. 10 Chochote mkono wako
unakifanya, kifanye kwa nguvu zako kwa sababu hakuna kazi, au ufafanuzi au ujuzi
au hekima katika Sheol, unapoenda. 11 Nimeona baadhi ya vitu vyakuvutia chini ya
jua: Mashindano hayatokani na watu wenye mbio. Vita havitokani na watu imara.
Mkate hautokani na watu wenye busara. Mali hazitokani na watu wenye ufahamu.
Kibali hakitokani na watu wenye ujuzi. Badala yake muda na bahati huwaathiri
wao wote. 12 Kwa kuwa hakuna anaye fahamu wakati wake wa kufa, kama vile
samaki wanaswavyo katika nyavu ya kifo, au kama vile ndege akamatwavyo katika
mtego. Kama wanyama wanadamu wamefungwa katika nyakati mbaya ambazo
ghafla huwaangukia. 13 Pia nimeona hekima chini ya jua kwa namna ambayo kwangu
ilionekana kubwa. 14 Kulikuwa na mji mdogo na watu wachache ndani yake, na
mfalme mkuu akaja kinyume na mji huo na akauzingira na akajenga mahandaki
kwa ajili ya kuushambulia. 15 Na katika mji kulikuwa na masikini, mtu mwenye
hekima, ambaye kwa hekima yake aliuokoa mji. Ila baadaye aliye mkumbuka yule
masikini. 16 Hivyo, nikasema, "Hekima ni bora kuliko nguvu, lakini hekima ya mtu
masikini hudharauliwa, na maneno yake hayasikilizwi." 17 Maneno ya watu wenye
hekima yaliongewa polepole yanasikiwa vizuri kuliko makelele ya mtawala yeyote
miongoni mwa wapumbavu. 18 Hekima ni bora kuliko silaha za vita, lakini mwenye
dhambi mmoja anaweza kuharibu mazuri mengi.

# 10

1 Kama nzi walio kufa husababisha manukato kutoa harufu ya uozo, hivyo
hivyo upumbavu kidogo hushinda hekima na heshima. 2 Moyo wa mtu mwenye
hekima huelekea kulia, lakini moyo wa mpumbavu huelekea kushoto. 3 Wakati
mpumbavu anapotembea barabarani, fikira zake zina upungufu, ikithibitisha kwa
kila mtu kwamba ni mpumbavu. 4 Kama jaziba za mtawala zikiinuka kinyume na
wewe, usiache kazi yako. Utulivu unaweza kutuliza ukatili mkubwa. 5 Kuna uovu
niliouona chini ya jua, aina ya kosa ambalo huja kutoka kwa mtawala: 6 Wapumbavu
wanapewa nafasi za uongozi, wakati watu walio faulu wanapewa nafasi za chini.
7 Nimewaona watumwa wakipanda farasi, na watu walio faulu wakitembea kama

watumwa juu ya ardhi. 8 Yeyote anayechimba shimo anaweza kutumbukia yake,
na popote mtu anayevunja ukuja, nyoka anaweza kumuuma. 9 Yeyote achongaye
mwawe, anaweza kuumizwa nayo. Na mtu achongaye mbao, anaweza kujihatarisha
kwa hiyo. 10 Kama chuma bapa kisicho na makali, na mtu hainoi, kisha ni lazima
atumie nguvu nyingi, lakini hekima hutoa faida kwa ufaulu. 11 Kama nyoka akiuma
kabla hajafurahi, hivyo hakuna faida kwa mfurahishaji. 12 Maneno ya kinywa cha
mtu mwenye hekima yana huruma. Lakini midomo ya mpumbavu humumeza
mwenyewe. 13 Kama maneno yanavyo anza kutiririka mdomoni mwa mpumbavu,
ujinga hutoka, na mwisho mdomo wake hutiririka wazimu mbaya. 14 Mpumbavu
huongeza maneno, lakini hakuna ajuaye kinachokuja. Ni nani ajuaye baada yake?
15 Jasho la wapumbavu huwavaa wao, hivyo hawajui hata barabara ya kwenda
mjini. 16 Ole wako ardhi kama mfalme wako ni kijana mdogo, na kama viongozi
wako huanza karamu ahsubuhi! 17 Lakini umebarikiwa ardhi kama mfalme wako
ni mwana wa waungwana, na kama vingozi wako hula wakati muafaka, kwa nguvu,
na sio kwa ulevi. 18 Kwa sababu ya uvivu paa huanguka. Na kwa sababu isiyo fanya
kazi nyumba hupata ufa. 19 Watu huandaa chakula kwa kicheko, divai huleta furaha
maishani, na fedha hutimiza hitaji kwa kila kitu. 20 Usimlaani mfalme, hata katika
akili, na usiwalaani wenye mali katika chumba chako cha kulala. Kwa kuwa ndege
wa angani inaweza kuchukua maneno yako. Chochote kilicho na mabawa kinaweza
kusambaza jambo.

# 11

1 Peleka mkate wako juu ya maji, kwa kuwa utaupata tena baada ya siku nyingi.
2 Shiriki mkate na watu saba, hata wanane kwa kuwa haujui ni majanga gani
yanayo kuja juu ya nchi. 3 Kama mawingu yamejaa mvua, yanajivua yenyewe chini
ya nchi. Na kama mti ukianguka kuelekea kusini au kuelekea kaskazini, popote
mti unapoangukia papo hapo utabakia. 4 Yeyote autazamaye upepo yawezekana
asipande, na yeyote atazamaye mawingu yawezekana asivune. 5 Kama usivyo jua njia
ya upepo, wala vile ambavyo mtoto akuavyo tumboni, vivyo hivyo huwezi kuielewa
kazi ya Mungu, aliye umba kila kitu. 6 Asubuhi panda mbegu yako; hadi jioni, fanya
kazi kwa mikono yako kama inavyo hitajika kwa kuwa haujui ni ipi itafanikiwa, jioni
au asubuhi, au hii au ile au zote zitakuwa nzuri. 7 Kweli nuru ni tamu, na ni kitu
cha kufurahisha kwa ajili ya macho kuona jua. 8 Kama mtu akiishi miaka mingi,
na aifurahie yote, lakina na afikiri juu ya siku zijazo za giza, kwa kuwa zitakuwa
nyingi. Kila kitu kijacho ni mvuke unaoteketea. 9 Furahia kijana, katika ujana wako,
na moyo wako ufurahie siku za ujana wako. fuatilia yale mema ya moyo wako,
chochote kilicho mbele ya macho yako. Ingawa, fahamu kwamba MUngu atakuleta
hukumuni kwa ajili ya vitu hivi vyote. 10 Ondoa hasira kutoka moyoni mwako, na
usijali maumivu yoyote katika mwili wako, kwa sababu ujana na nguvu zake ni
mvuke.

# 12

1 Pia mkumbuke Muumba wako katika siku za za ujana, kabla ya siku za ugumu
hazijaja, na kabla ya miaka haijafika utakapo sema, “Mimi sina furaha katika
hizo,” 2 fanya hivi kabla ya nuru ya jua na mwezi na nyota havijawa giza, na
mawingu kurudi baada ya mvua. 3 Huo utakuwa wakati ambapo mlinzi wa ikulu
atatetemeka, na wanaume imara wameinama, na wanawake wanao saga kukoma,
kwa sababu ni wachache, na wale wanao chungulia dirishani hawaoni vizuri tena.
4 Huo utakuwa wakati ambao milango imefungwa katika mtaa, na mlio wa kusanga
kukoma, wakati wanaume watasitushwa kwa mlio wa ndege, na wimbo wa sauti
ya wasichana kukoma. 5 Utakuwa wakati ambapo watu wataogopa vilivyoinuka na

hatari iliyoko barabarani, na wakati ambapo mlozi utachanua maua, na wakati panzi
watakapokokotana wenyewe, na wakati ambapo hamu za asili zitakaposhindwa.
Kisha mtu aenda katika nyumba yake ya milele na waombolezaji watelemka mitaani.
6 Mkumbuke Muumba wako kabla ya kamba ya fedha kukatwa, au bakuli ya dhahabu
kupasuka, au gudulia kuvunjwa kwenye chemuchemi, au torori la maji kuvunjika
kisimani, 7 kabla mavumbi kurudia mahali yalipotoka, na roho kurudi kwa Mungu
aliyeitoa. 8 Kama ukungu wa mvuke," asema mwalimu, kila kitu ni mvuke upoteao.
9 Mwalimu alikuwa na hekima na aliwafundisha watu maarifa. Alisoma na kuazimu
na kutunga mithali nyingi katika mpangilio. 10 Mwalimu alitafuta kuandika kwa
kutumia vithibitisho dhahiri, maneno ya kweli yaliyo wima. 11 Maneno ya watu
wenye hekima ni kama mchokoo. Kama misumari ilivyogongomewa kwa undani,
ndivyo yalivyo maneno ya mabwana katika mkusanyiko wa mithali zao, ambayo
yamefundishwa na mchungaji mmoja. 12 Mwanangu kuwa makini na kitu zaidi,
utengezaji wa vitabu vingi, ambacho hakina mwisho, na kusoma kwingi huleta
uchovu mwilini. 13 Mwisho wa jambo baada ya kila kitu umesikika, ni kwamba ni
lazima umche Mungu na kushika amri zake, kwa kuwa huu ndilo jukumu lote la
mwanadamu. 14 Kwa kuwa Mungu ataleta kila tendo hukumuni, pamoja na kila kitu
kilichofichika, kizuri au kibaya.

# Wimbo wa Sulemani

[1] Wimbo ulio Bora, ambao ni wa Sulemani. Wanamke mdogo akizungumza
na mpenzi wake [2] O, laiti ungenibusu na mabasu ya mdomo wako, kwa kuwa
upendo wako ni bora kuliko mvinyo. [3] Mafuta yako ya upako yana manukato
mazuri; jina lako ni kama marashi yaeleayo, hivyo wanawake wadogo wanakupenda.
[4] Nichukuwe kwako, na tutakimbia. Mwanamke akizungumza mwenyewe Mfalme
amenipeleka vyumbani mwake. Mwanamke akizungumza na mpenzi wake nina
furuha; nina furahi kuhusu wewe; acha ni shereheke upendo wako; ni bora kuliko
mvinyo. Ni halisi kwa wanawake wengine kupenda. Mwanamke akizungumza na
wanawake wengine. [5] Mimi ni mweusi lakini mzuri, enyi mabinti wa wanaume wa
Yerusalemu - mweusi kama hema za Kedari, muzuri kama mapazia ya Sulemani.
[6] Usinishangae kwasababu ni mweusi, kwasababu jua limeniunguza. Wana wa
mama yangu walikuwa na hasira juu yangu; walinifanya mtunzi wa mashamba ya
mizabibu, lakini mshamba langu la mizabibu sijatunza. Wanamke akizungumza na
mpenzi wake. [7] Niambie, wewe ninaye kupenda, wapi unalisha mifugo yako? Wapi
unapumzisha mifugo yako mchana? Kwa nini niwe kama mtu anaye akangaika
miongoni mwa mifugo ya marafiki zako? Mpenzi wake anamjibu [8] Kama haujui,
uliye mzuri miongoni mwa wanawake, fuata nyayo za mifugo yangu, na ulishe watoto
wako wa mbuzi karibu na hema za wachungaji. [9] Nina kulinganisha, mpenzi wangu,
na farasi mzuri wakike miongoni mwa farasi wa magari ya Farao. [10] Mashavu
yako ni mazuri na mapambo, shingo yako na mikufu ya madini. [11] Nitakufanyia
mapambo ya dhahabu yaliochanganywa na fedha. Mwanamke akiongea mwenyewe.
[12] Wakati mfalme akiwa amelala kitandani mwake, marashi yangu yakasambaza
arufu. [13] Mpenzi wangu ni kwangu kama mkebe wa marashi unao lala usiku katika
ya maziwa yangu. [14] Mpenzi wangu ni kwangu kama kifurushi cha maua ya hena
katika mashamba ya mizabibu ya Eni Gedi. Mpenzi wake anazungumza naye [15] Ona,
wewe ni mzuri, mpenzi wangu; ona, wewe ni mzuri; macho yako ni kama ya hua.
Mwanamke anazungumza na mpenzi wake. [16] Ona, wewe ni mtanashati, mpenzi
wangu, jinsi mtanashati. [17] Nguzo za nyumba yetu ni za matawi ya mierezi, na dari
letu ni la matawi ya miberoshi.

## 2

[1] Mimi ni ua katika tambarare, nyinyoro katika bonde. Mwanaume akizungumza
naye [2] Kama nyinyoro miongoni mwa mimba, ndivyo wewe, mpenzi wangu,
miongoni mwa mabinti wengine wote. Mwanamke akizungumza mwenyewe [3] Kama
mti wa mpera ulivyo miongoni mwa miti ya misituni, ndivyo mpenzi wangu alivyo
miongoni mwa wanaume. Nina kaa chini ya kivuli chake kwa furaha sana, na tunda
lake ni tamu kwa ladha yangu. [4] Amenileta kwenye ukumbi wa maakuli, na bendera
yake juu yangu ilikuwa upendo. Mwanamke akizungumza na mpenzi wake. [5] Ni
uishe kwa keki za mizabibu na kuniuisha na mapera, kwa kuwa nimedhohofika
na mapenzi. Mwanamke akizungumza mwenyewe [6] Mkono wake wakushuto upo
chini ya kichwa changu, na mkono wake wa kulia wanikumbatia. Mwanamke
akizungumza na wanawake wengine. [7] Ninataka muhaidi, mabinti wa Yerusalemu,
kwa swala na paa wa porini, kwamba hamtavuruga mapenzi yetu hadi yatakapo
isha yenyewe. Mwanamke akizungumza mwenyewe. [8] Sauti ya mpenzi wangu hiyo!
O, huyu yuwaja, akiruka ruka juu milima, akiruka vilimani. [9] Mpenzi wangu ni
kama swala au mtoto mdogo wa paa; angalia, amesimama nyuma ya ukuta wetu,

akishangaa kupitia dirishani, akichungulia wavuni. 10 Mpenzi wangu alizungumza
na mimi na kusema, “Amka, mpenzi wangu; mzuri wangu, twende pamoja nami.
11 Angalia, baridi imepita; mvua imeisha na kwenda. 12 Maua yametokeza juu ya
nchi; wakati wa kupunguza matawi na kuimba kwa ndege umekuja, na sauti za
hua zimesikika nchini kwetu. 13 Mti wa tini umepevusha tini zake za kijani, na
mizabibu imestawi; yatoa marashi yake. Inuka, mpenzi wangu, mzuri wangu, na uje
nami. 14 Hua wangu, katika miamba ya mawe, katika miamba ya siri ya mipasuko
ya milima, acha nione uso wako. Acha nisikie sauti yako, kwa kuwa sauti ni tamu,
na uso wako ni mzuri.” Mwanamke akiongea mwenyewe 15 Wakamate mbweha kwa
ajili yetu, mbweha wadogo wanao haribu shamba za mizabibu, kwa kuwa shamba
la mizabibu limestawi. 16 Mpenzi wangu ni wangu, na mimi ni wake; anakula penye
nyinyoro kwa raha. Mwanamke anaongea na mpenzi wake 17 Enenda zako, mpenzi
wangu, kabla pepo za jioni hazija vuma na vivuli kutoweka. Nenda zako; kuwa kama
ayala au mtoto mdogo wa paa katika milima mawe mengi.

# 3

1 Usiku katika kitanda changu nilikuwa na shauku ya yeye ni mpendaye;
nilimtafuta, lakini sikumpata. 2 Nilisema binafsi, “Nitainuka na kwenda kupitia mji,
kupitia mitaa na sokoni; nitamtafuta.” Nilimtafuta, lakini sikumpata. 3 Walinzi
walinipata walipo kuwa doria katika mji. Nikawauliza, “Mmemuona mpenzi
wangu?” 4 Ni baada ya mda mfupi kupita nilipo wapita nikampata ninaye mpenda.
Nilimshika na sikumuacha hadi nilipo mleta nyumbani mwa mama yangu, katika
chumba cha yeye aliyenichukua mimba. Mwanamke akiongea na wanawake
wengine. 5 Ninataka muape, mabinti wa wanaume waYerusalemu, kwa ayala na
paa wa porini, kuwa hamtavuruga mapenzi yetu hadi yatakapo isha yenyewe.
Mwanamke mdogo akizungumza mwenyewe 6 Nini hiyo inayo toka nyikani kama
nguzo za moshi, umefukizwa manemane na ubani, pamoja na unga wote wa
manukato unao uzwa na wafanya biashara? 7 Angalia, nikitanda cha Sulemani;
mashujaa sitini wamekizunguka, wanajeshi elfu sitini wa Israeli 8 Wao ni wazoefu
wa upanga na wanaujuzi wa vita. Kila mwanaume ana upanga wake pembeni
yake, akijizatiti na maasi ya usiku. 9 Mfalme Sulemani akajijengea kiti cha kifalme
cha kubebwa na mbao za Lebanoni. 10 Nguzo zake zilijengwa kwa fedha; nyuma
kuliekwa dhahabu, na kiti kitambaa cha zambarau. Ndani mwake kulipambwa na
upendo na mabinti wa wanaume wa Yerusalemu. Mwanamke mdogo akizungumza
na wanawake wa Yerusalemu 11 Nenda nje, mabinti wa wanaume wa Sayuni, na
mtazame mfalme Sulemani, akivikwa taji ambalo mamaye alimvika siku ya arusi
yake, katika siku ya furaha ya maisha yake.

# 4

1 O, wewe ni mzuri, mpenzi wangu; wewe ni mzuri. Macho yako ni ya hua nyuma
kitamba chako cha uso. Nywele zako ni kama kundi la mbuzi likienda chini kutoka
Mlima Gileadi. 2 Meno yako ni kama kondoo walio nyolewa, wakitoka sehemu ya
kuoshwa. Kila mmoja ana pacha, na hamna ata mmoja miongoni mwao aliyefiwa.
3 Mdomo wako ni kama uzi mwekendu; mdo wako wapendeza. Mashavu yako ni
kama majani ya komamanga nyuma ya kitambaa chako cha uso. 4 Shingo yako
ni kama mnara wa Daudi ukiwa umejengwa kwa mistari ya mawe, na ngao elfu
moja ikining'nia juu yake, ngao zote za wanajeshi. 5 Maziwa yako mawili ni kama
swala wawili, mapacha wa ayala, wakila miongoni mwa nyinyoro. 6 Hadi jioni ifike
na vivuli viondoke, nitaenda kwenye mlima wa manemane na vilima vya ubani.
7 Wewe ni mzuri kwa kila namna, mpenzi wangu na hakuna lawama ndani yako.

8 Njoo nami kutoka Lebanoni, bibi arusi wangu. Njoo nami kutoka Lebanoni; njoo
kutoka juu ya Amana, kutoka juu ya Seneri na Herimoni, kutoka shimoni mwa simba,
kutoka mashimo ya milima ya chuwi. 9 Umeuiba moyo wangu, dada yangu, bibi arusi
wangu; umeuiba moyo wangu, kwa mtazamo mmoja tu wako kwangu, kwa mkufu
mmoja wa shingo yako. 10 Jinisi gani upendo wako ulivyo mzuri, dada yangu, bibi
arusi wangu! Jinsi gani zaidi upendo wako ulivyo bora kuliko mvinyo, na arufu ya
marashi yako kuliko manukato yeyote. 11 Midomo yako, bibi arusi wangu, yatiririka
asali; asali na maziwa vichini ya ulimi wako; arufu ya mavazi yako ni kama marashi
ya Lebanoni. 12 Dada yangu, bibi arusi wangu ni bustani ilio fungwa, bustani ilio
fungwa, chemchemi iliyo fungwa kwa muhuri. 13 Matawi yako ni kichaka cha miti
ya komamanga yenye matunda tofauti, na ya mimea ya hina na nardo, 14 Nardo na
Zafarani, mchai na mdalasini pamoja na aina zote za uvumba, manemane na udi na
aina tofauti za manukato. 15 Wewe ni bustani ya chemchemi, kisima cha maji safi,
mifereji inayo shuka kutoka Lebanoni. Mwanamke mdogo akizungumza peke yake
16 Amka, upepo wa kaskazini; njoo, upepo wa kusini; vuma katika bustani yangu ili
manukato yake yatoe marashi. Mpenzi wangu na aje katika bustani yake na kula
matunda ya chaguo lake.

# 5

1 Nimekuja katika bustani yangu, dada yangu, bibi arusi wangu; Nimekusanya
udi wangu na manukato yangu. Nimekula mziga wangu wa asali na asali yangu;
Nimekunywa mvinyo wangu pamoja na maziwa yangu. Marafiki wanazungumza
na wapenzi Kuleni, marafiki; kunyweni na mlewe na mapenzi. Mwanamke mdogo
akizungumza mwenyewe 2 Nilikuwa nimelala, lakini moyo wangu ulikuwa umeamka
katika ndoto. Sauti ya mpenzi wangu yabisha na kusema, “Nifungulie, dada yangu,
mpenzi wangu, hua wangu, wangu usiye na doa, kwa kuwa kichwa changu kimelowa
na matone, nywele zangu na unyevu wa usiku.” 3 “Nimevua joho langu; lazima
nilivae tena? Nimeosha miguu yangu; lazima ni ichafue?” 4 Mpenzi wangu anaeka
mkono wake kwenye kitasa, na moyo wangu ukawaka kwa ajili yake. 5 Nimeamka
kumfungulia mlango mpenzi wangu; mikono yangu ikawa yamiminika na udi, vidole
vyangu na unyevu wa udi, katika komeo la mlango. 6 Nimemfungulia mlango mpenzi
wangu, lakini mpenzi wangu aligeuka na kwenda. Moyo wangu ukadididimia; nikakosa
tumaini. Nikamtafuta, lakini sikumpata; nikamuita, lakini hakunijibu. 7 Walinzi
waliokuwa wakizunguka mjini walinipata mimi; walinipiga chini na kunijeruhi;
askari katika ukuta walichukua nguo yangu ya juu. Mwanamke mdogo akizungumza
na wanawake wa mji 8 Ninataka uhaidi, mabinti wa Yerusalemu, kwamba mkimuona
mpenzi wangu, mwambie ninaumwa sababu ya upendo wangu kwake. Wanawake
wa mji wakizungumza na mwanamke mdogo 9 Mpenzi wako ana ubora gani kuliko
mwanaume mwengine, wewe uliye mzuri miongoni mwa wanawake? Kwanini
mpenzi wako bora kuliko mpenzi mwengine, hadi utuulize tuweke nadhiri kama hii?
Mwanamke mdogo akizungumza na wanawake wa mji 10 Mpenzi wangu amenawiri
na ana ng'aa, kati ya wanaume elfu kumi. 11 Kichwa chake ni dhahabu safi; nywele
zake ni laini na nyeusi kama kunguru. 12 Macho yake ni kama ya hua pembezoni
ya vijito vya maji, yameoshwa na maziwa, yameundwa kama mikufu. 13 Mashavu
yake ni kama vitanda vya manukato, vinavyotoa arufu ya marashi. Midomo yake
nni nyinyoro, inayo tiririka udi. 14 Mikono yake ni ya mianzi ya dhahabu iliyo
zungushiwa mikufu; tumbo lake ni pembe lililo funikwa yakuti samawi. 15 Miguu
yake ni nguzo za marimari, iliyo ekwa juu ya dhahabu safi; muonekano wake ni
kama Lebanoni, mizuri kama mierezi. 16 Mdomo wake ni mtamu; ni mzuri sana.
Huyu ni mpenzi wangu, na huyu ni rafiki yangu, mabinti wa Yerusalemu.

# 6

1 Mpenzi wako ameenda wapi, ulio mzuri miongoni mwa wanawake? Kwa njia
gani mpenzi wako ameenda? ilitumtafute nawe? Mwanamke mdogo akizungumza
mwenyewe 2 Mpenzi wangu ameenda katika bustani yake, kwenye vitanda vya
manukato, kwenda kula katika bustani na kukusanya nyinyoro. 3 Mimi ni wa mpenzi
wangu, na mpenzi wangu ni wangu; na kula katika nyinyoro kwa raha. Mpenzi
wa mwanamke akizungumza naye 4 Wewe ni mzuri kama Tirza, mpenzi wangu,
wapendeza kama Yerusalemu, waamasisha kama jeshi lenye bendera mbele. 5 Geuza
macho yako mbali na mimi, kwa kuwa yana nizidi ukali. Nywele zako ni kama
kundi la mbuzi likishuka chini kutoka miteremko ya Mlima Gileadi. 6 Meno yako ni
kama kundi la kondoo likishuka kutoka sehemu ya kuoshwa. Kila mmoja anapacha,
na hamna ata mmoja aliyefiwa. 7 Mashavu yako ni kama majani ya komamanga
nyuma ya kitambaa chako cha uso. Mpenzi wa mwanamke akizungumza peke yake
8 Kuna malikia sitini, masuria themanini, na wanawake wadogo bila idadi. 9 Hua
wangu, asiye na doa wangu, ni yeye pekee; ni binti muhimu wa mama yake; ndiye
kipenzi cha mwanamke aliye mzaa. Mabinti wa wenzengu wamemuona na kumuita
mbarikiwa; wamalikia na masuria walimuona pia, na wakamsifu: Kile walicho
sema wamalikia na masuria 10 “Ni nani huyo anaye jitokeza kama kukicha, mzuri
kama mwezi, ana ng'aa kama jua, uamasisha kama bendera ya jeshi?” Mpenzi wa
mwanamke akizungumza mwenyewe 11 Nimeenda kwenye kichaka cha miti ya milozi
kuona mimea midogo ikikua bondeni, kuona kama mizabibu imechipua, na kama
mikomamanga imestawi. 12 Nilikuwa nina furaha nikahisi kama nimepakia gari ya
farasi la mtoto wa mfalme. Mpenzi wa mwanamke akizungumza naye 13 Geuka
nyuma, geuka nyuma, wewe mwanamke mkamilifu; geuka nyuma, geuka nyuma
iliniweze kukushangaa. Mwanamke mdogo akizungumza na mpenzi wake Kwanini
wanishangaa, mwanamke mkamilifu, kana kwamba nina cheza katika ya mistari
miwili ya wachezaji?

# 7

1 Jinsi gani miguu yako ilivyo yaonekana mizuri kwenye viatu, binti wa mfalme!
Mapaja yako ni kama mikufu, kama kazi ya mjenzi. 2 Kitovu chako ni kama duara la
bakuli; kamwe kisikose mchanganyiko wa mvinyo. Tumbo lako ni kama ngano iliyo
umuka na kuzungushiwa nyinyoro. 3 Maziwa yako mawili ni kama watoto wawili
wa ayala, mapacha wa ayala. 4 Shingo yako ni kama mnara wa pembe; macho
yako ni kama maziwa ya Heshiboni kwenye lango la Bathi Rabimu. Pua yako ni
kama mnara wa Lebanoni ambao watazama Damasko. 5 Kichwa chako ni kama
Karmeli; nywele kichwani mwako ni za zambarau nyeusi. Mfalme amestaajabishwa
na vifundo vyake vya nywele. 6 Jinsi gani ulivyo mzuri na wakupendeza, mpenzi,
na mazuri yako. 7 Urefu wako ni wa kama mti wa mtende, na maziwa yako kama
vifungu vya matunda. 8 Niliwaza, “Ninataka kuupanda huo mti wa mtende; nitashika
matawi yake.” Maziwa yako nayawe kama vifungu vya mizabibu, na harufu ya
pua yako yawe kama mapera. 9 Mdomo wako na uwe kama mvinyo bora, ukishuka
taratibu kwa mpenzi wangu, ukiteleza kwenye midomo yetu na meno. Mwanamke
mdogo akizungumza mwenyewe 10 Mimi ni wa mpenzi wangu, na ananitamani.
11 Njoo, mpenzi wangu, twende nje ya mji; tu lala usiku kwenye vijiji. 12 Tuamke
mapema twende kwenye mashamba ya mizabibu; tuone kama mizabibu imemea,
kama imechipua, na kama mikomamanga imetoa mau. Pale nitakupa penzi langu.
13 Mitunguja ya toa harufu yake; katika mlango wa tunapoishi kuna kila aina ya
matunda, mpya na ya kale, niliyo kuhifadhia, mpenzi wangu.

# 8

1 Ninatamani ungekua kama kaka yangu, aliye nyonya ziwa la mama yangu. Ili
kwamba kila ningekuona nje ningekubusu pasipo mtu kunidharau. 2 Nitakuongoza
na kukuleta kwenye nyumba ya mama yangu, na utanifundisha. Nitakupa mvinyo
ulio chachwa unywe na baadhi ya jwisi ya komamanga. Mwanamke mdogo
akizungumza mwenyewe 3 Mkono wake wa kushoto uko chini ya kichwa changu
na mkono wake wa kulia wanikumbatia. Mwanamke akiongea na wanawake
wengine 4 Ninataka muape, mabinti wa wanaume wa Yerusalemu, kuwa ham-
tavuruga mapenzi yetu hadi yatakapo isha yenyewe. Wanawake wa Yerusalemu
wakizungumza 5 Ni nani huyu anaye kuja kutoka nyikani, amemuegemea mpenzi
wake? Mwanamke mdogo akizungumza na mpenzi wake nimekuamsha chini ya
mti wa mpera; pale mama yako alichukua mimba; pale alikuzaa, alijifungua wewe.
6 Nieka kama muhuri kwenye moyo wako, kama muhuri kwenye mkono wako,
kwa kuwa mapenzi yana nguvu kama mauti. Mapenzi mazito hayana kurudi
kama kwenda kuzimu; miale yake yalipuka; ni miale ya moto inayo waka, miale
yenye joto kuliko moto wowote. 7 Maji yalio zuka hayawezi kuzimisha upendo,
wala mafuriko hayawezi kuondoa. Mwanaume akitoa mali zake zote kwa ajili ya
upendo, ukarimu wake utadharauliwa. Kaka zake mwanamke mdogo wakizungumza
wenyewe 8 Tuna dada mdogo, na matiti yake bado hayajakua. Nini tutamfanyia
dada yetu siku hatakayo ahidiwa kuolewa? 9 Kama ni ukuta, tutamjengea juu
yake mnara wa fedha. Kama ni mlango, tutampamba kwa mbao za mierezi.
Mwanamke mdogo akizungumza peke yake 10 Nilikuwa ukuta, lakini matiti yangu
sasa ni kama nguzo imara; hivyo nimekomaa machoni pake. Mwanamke mdogo
akizungumza mwenyewe 11 Sulemani alikuwa na shamba la mizabibu huko Baali
Hamoni. Aliwakodishia wao ambao watalitunza. Kila mmoja alipaswa kuleta shekeli
elfu moja za fedha kwa matunda yake. 12 Shamba langu ka mzabibu ni langu, shekeli
elfu moja ni za kwako, Sulemani mpenzi, na shekeli mia mbili ni za wale wanao tunza
matunda yake. Mpenzi wa mwanamke akizungumza naye. 13 Wewe unaye ishi katika
bustani, marafiki zangu wanasikiliza sauti yako; acha na mimi niweanaye isikia pia.
Mwanamke mdogo akiongea na mpenzi wake 14 Harakisha, mpenzi wangu, na uwe
kama paa au mtoto wa paa kwenye milima ya manukato.

# Isaya

[1] Maono ya Isaya mtoto wa Amozi ambayo aliyaona kuhusu Yuda na Yerusalemu
katika vipindi vya utawala wa Uzia, Yothamu, Ahazi, na Hezekia, wafalme wa
Yuda. [2] Sikia enyi mbingu, tega sikio ewe nchi; kwa kuwa Yahwe amesema:
''Nimewatunza na kuwalea watoto, lakini wamenigeuka. [3] Ng'ombe anamjua
anayemmiliki na punda anajua sehemu anapowekewa chakula, lakini Israeli hawajui,
wala hawafahamu.'' [4] Ole! Taifa, wenye zambi, mtu muovu, watoto wa wenye
zambi, watoto wanaoenda kinyume, Wamemtelekeza Yahwe, wamedharau aliye
Mtakatifu wa Israeli, wamejitenga wenyew kutoka kwake. [5] Kwa nini ulikuwa
unaendelea kupigwa? Kwa nini unazidi kuasi zaudi na zaidi? Kichwa chote kinauma,
moyo wote ni dhaifu. [6] Kutoka kwenye unyayo wa mguu mpaka kichwani kila
sehemu ina maumivu; ni madonda na majeraha mabichi yaliyoachwa wazi, ambayo
hayajafungwa, kuasifishwa, kuwafunga vidonda vyao, wala kuwaponya kwa mafuta.
[7] Nchi yenu imeharibiwa; miji yenu imechomwa moto; mashamba yenu— mbele,
wageni wamehiaribu; wamepatelekeza katika uharibifu, ulioangushwa na wageni
[8] Binti Sayuni ameacha kama kibanda katika shamba la mzabu, kama kivuli kitika
shamba la matango, kama mji unaomba. [9] Kama Yahwe wa majeshi hakutuasha kwa
mda mfupi tungekuwa kama Sodoma, tungekuwa kama Gomora. [10] Sikiliza neno la
Yahwe, enyi viongozi wa Sodomu; sikilizeni sheria ya Mungu wetu, enyi watu wa
Gomora: [11] ''Sadaka zenu ni nyingi kiasi gani kwangu?'' asema Yahwe. ''Nimesikia
vya kutosha kuhusu sadaka yenu ya mwana kondoo, na mnyama alionona; na
damu ya ng'ombe, ndama, au mbuzi si vifurahii. [12] Ulipokuja kuonekaa mbele
yangu, Ni nani aliyehitaji hili juu yako, kukanyaga katika mahama yangu [13] Msilete
tena sadaka zisizo na maana; maana zinaniongezea uchafu mmekusanyika katika
siku yenu mpya ya mwenzi na sabato—Mimi siwezi vumlia mikusanyio hii ya
waovu. [14] Ninaichukia sherehe yenu mpya ya mwenzi na sherehe zilizoteuliwa;
ni mzigo kwangu; nimechoka kuubeba. [15] Hivyo basi mnapotawanya mikono yenu
kitkika maombi, sitawangalia hata kama mkiomba sana, sitawasikiliza; mikono yenu
imejaa damu. [16] Jiosheni, jitakaseni wenyewe; ondoeni matendo maovu mbele ya
macho yangu; acheni kutenda dhambi; [17] jifunze kutenda mema; tafuta ukweli;
msiwanyanyase, wapeni haki yatima, walindeni wajane.'' [18] Njooni sasa, njooni
tusemezane, asema Yahwe, japokuwa dhambi zenu ni nyekundu kama bendera
zitakuwa nyeupe kama theluji; japokuwa ni myekundu kama damu zitakuwa kama
sufi. [19] Kama utakubali na kutii, utakula mema ya nchi, [20] lakini ukikataa na
kugeuka, upanga utakuangamiza, maama Yahwe amesema. [21] Ni kwa jinsi gani mji
ulioaminika umekuwa kahaba! ulikuwa ni mij wenye usawa na haki, lakini sasa mji
umejaa mauwaji. [22] Fedha zenu zimechafuka, na mvinyo wenu umechanganjwa na
maji. [23] Viongozi wenu wamemgeuka Mungu wamekuwa marafiki wa wezi; yeyote
anayopenda rushwa na kuikimbilia. Hawawajali yatima, wala wajane wanaokuja
kuwanyenyekea mbele yao. [24] Hivyo basi hili ndilo tamko la Bwana, Yahwe wa
majeshi, Shujaa wa Israeli: Ole wao! nitachukua hatua kwa wale walio kinyume
na mimi na niwaadhibu wale wanaonipinga; [25] Nitaugeuza mkono wangu juu yako,
nitatakasa chuma kilicho chakaa na kuondoa kutu yote. [26] Nitailinda hukumu yako
kama ilivyokuwa mwanzo, na washauri wako kama ilivyokuwa hapo mwanzo; baada
ya hapo mtaitwa mji wa haki, mji wa imani.'' [27] Sayuni itakombolewa kwa haki, na
wanaotubu kwa haki. [28] Waasi na wenye dhambi wataangamizwa pamoja, na wale
wataenda kinyume na Yahwe watauliwa. [29] Kwakukuwa utaona aibu juu ya miti

ya mialoni uliyoitamani, na utakuwa na hofu juu ya bustani uliyoichagua. 30 Kwa
kukuwa utakuwa kama mualoni ambao majani yake yamenyauka, na kama bustani
isiyokuwa na maji. 31 Mtu mwenye nguvu atakuwa kama kitu kikavu, na kazi yake
itakuwa kama cheche; zitawaka moto kwa pamoja, na hakuna hata mmoja ataweza
kuuzima''.

# 2

1 Vitu ambavyo Isaya mtoto Amozi alivijua katika maono, kuhusu Yuda na
Yerusalemu. 2 Na itakuwa katika siku za mwisho, ule mlima wa nyumba ya Yahwe
itaanzishwa kama mlima mrefu zaidi, na utanyanyuliwa juu ya vilima, na mataifa
yote yatakusanyika pale. 3 Watu wengi watakuja na kusema, ''Njooni, twendeni juu
ya mlima wa Yahwe, kwenye nyumba ya Mungu wa Yakobo, kwa hiyo anaweza
kutufundisha baadhi ya njia zake na tunaweza kutembea katika njia zake.'' Nje
ya Sayuni itaenda sheria na neno la Yahwe litatoka Yerualemu. 4 Atahukumu kati
ya mataifa na atatoa maamuzi kwa watu wote; watayapiga nyungo mapanga yao
kuwa majembe, na mikiku yao kama ya kukatia ndoano; taifa halitanyanyua upanga
juu ya taifa lingine, na wala hawata jiandaa kwa vita tena. 5 Nyumba ya Yakobo,
njooni, na tutembee katika mwanga wa Yahwe. 6 Kwa maana mmewatekeleza watu
wenu, nyumba ya Yakobo, wamejazwa na desturi kutoka mashariki na dalili kutokea
kama mfilisti, na watasalimiana kwa mikono na wana wa wageni. 7 Nchi yao
imejaa fedha na dhahabu, na hakuna mipaka katika utajiri wao; nchi yao pia imejaa
farasi, wala hakuna mipika ya magari. 8 Nchi yao pia imejaa sanamu; wanaabu
utengenezaji wa mikono yao wenyewe, vitu aambavyo vidole vyao vimetengeneza.
9 Watu watainama chini, na kila mmoja atanguka chini; hivyo basi msiwanyanyue
juu. 10 Nendeni maeneo yenye miamba na mjifiche kwenye aridhi kwa hofu ya Yahwe
na kwa utukufu wa enzi yake. 11 Mtu anaye tazama kwa kujivuna atashushw chini,
na kiburi cha watu kitashushwa chini, na Yahwe mwenyewe atainuliwa siku hiyo.
12 Maana kutakuwa na siku ya Yahwe wa majeshi juu ya yeyote anayejigamba na
kujiinua juu, na dhidi ya yeyote mwenye kiburi na atashushwa chini- 13 na dhidi ya
mierezi ya Lebanoni iliyo juu na kupandishwa juu, na dhidi ya mialoni ya Bashani.
14 Siku hiyo ya Yahwe wa majeshi itakuwa dhidi ya milima yote mirefu, na dhidi ya
vilima vyote vilivyonyanyuliwa juu, 15 na dhidi ya minara mirefu, na dhidi ya kila
ukutaunaojitokeza, 16 na dhidi ya merikebu zote za Tarshishi, na dhidi ya vyombo
vizuri vya meli. 17 Kiburi cha mwanaume kitashushwa chini, na kiburi cha wanaume
kitaanguka; Yahwe mwenyewe atainuliwa siku hiyo. 18 Sanamu zote zitaondolewa.
19 Wanaume wataingia kwenye mapango ya miamba na mashimo ya aridhi, kwa hofu
ya Yahwe, na kwa utukufu wa enzi yake, atakapo nyanyuka na kuitisha nchi. 20 Siku
hiyo watu watatupa sanamu zao za fedha na dhahabu ambazo wametengeneza
wenyewe kwa ajili ya kuabudia - watazitupa mbali kwa fuko na popo. 21 Watu
wataingia kwenye miamba kupitia mwanya itakuwa miamba chakavu, kwa hofu ya
Yahwe na utukufu wa enzi yake, 22 usimwaminia mtu, ambae pumzi yake inatokea
katika pua yake, ni kwa kiasi gan?

# 3

1 Ona, Bwana, Yahwe wa majeshi, anakaribia kuwachukua kutoka Yerusalema na
Yudawasaidizi na wafanyakazi: wasambazaji wote wa mikate, wasambazaji wote
wa maji; 2 mtu mwenye nguvu, shuja, hakimu, nabii, dalili za msomaji, na mzee;
3 naodha wa hamsini, raia husika, mshauri, fundi mtarajiwa, na mchawi stadi.
4 Nitamuweka kijana tu kama kiongozi wenu, kijana atawaongoza wao. 5 Watu
watanyanyasika, kila mmoja mmoja na kila mmoja na jirani yake; watoto watawatusi

wazee, na mivutano itawapa changamoto waheshimiwa. [6] Mwanaume atamshikilia
ndugu yake katika nyumba ya baba yake na kusema, 'Unayo kanzu; uwe kiongozi
wetu, na uharibifu huu uwe mikononi mwako. [7] 'Siku hiyo atapaza sauti na kusema,
'hautakuwa mganga; sina mkate wala mavazi. Hatanifanya kuwa kiongozi wa
watu. [8] Kwa maana Yerusalemu kuna mashaka, na Yuda imeanguka, kwa sababu
mazungumzo yao na matendo yao yako kinyume na Yahwe, wanayapinga macho
ya utukufu wake. [9] Angalia nyuso zao zinashudia kinyume nao; na watasema
dhambi zao kama Sodoma; hawatazificha, Ole wao! Maana wanakamilisha janga
lao wenyewe. [10] Mwambie mtu mwenye haki kwamba itakuwa vizuri, maana
watakula matunda ya matendo yao. [11] Ole kwa wakosaji! itakuwa vibaya kwa
yeye, maana malipo ya mikono yake yatafanyika kwake pia. [12] Watu wangu-watoto
wangu wanawakandamiza, na wanawake wanawaongoza wao. Watu wangu, wale
wanaowaongoza wanawaongoza vibaya na kuchanganya muelekeo wa nja yenu.
[13] Yahwe simama juu ya mashitaka; yeye amesimama kuwashaki watu. [14] Yahwe
atakuja na hukumu juu ya wazee na watu wao na viongozi wao: "Umeharibu shamba;
nyara kutoka kwa masikni ziko kwenye nyumba zako. [15] Kwa nini unaponda watu
wangu na kusaga nyuso za masikini?" Hili ni tamko Bwana, Yahwe wa majeshi.
[16] Yahwe anasema hivyo kwa sababu mabinti wa Sayuni wanajigamba, wanatembea
pekee yao vichwa vyao vikiwa juu, na kutaniana kwa macho yao, na kutakata kokote
waendako na kuamua upatu kwa miguu yao, [17] Kwa hiyo Bwana atafanya magonjwa
ya mapele kwenye kishwa cha mabinti wa Sayuni, na Yahwe atawafanya upaa.
[18] Siku hiyo Bwana ataondoa mapambo mazuri yaliyoko kwenye kifundo cha miguu,
bendi za kichwa chao, kaya zao; bangili za masikio, [19] bangili za miguu na taji zao;
[20] kitambaa cha kichwa, chaini za miguu, mafurungu na maboksi ya marashi na
na haiba ya bahati. [21] Atatoa bangili na kipini kwenye pua; [22] sherehe za mavazi,
mapazia na mabegi ya mkononi; [23] vioo vya mkononi, sanda nzuri, vilemba vya
kichwa na taji. [24] Badala ya manukato mazuri kutakuwa na arufu mbaya; na badala
ya ukunda, kamba, kufunika kwa vazi la gunia; kitia alama mwilini kwa moto badala
ya uzuri. wanaume wao wataanguka kwa upanga, [25] na wanaume wenye nguvu
wataanguka kwenye vita. [26] Lango la Yerusalemu litaomboleza na kuomboleza; na
atakuwa peke yake amekaa chini ya ardhi.

# 4

[1] Siku hiyo wanawake saba watamchukua mwanaume mmoja na kusema, "Tu-
takula chakula chetu wenyewe, tutavaa nguo zetu wenyewe. lakini tunahitaji
kuchukua jina lako ili tuondoe haibu zetu." [2] Na siku hiyo tawi zuri la Yahwe na
utukufu, na matunda yatakuwa na ladha nzuri na kupendeza kwa wale wanaoishi
Israeli. [3] Itatokea kwa yule aliyeachwa Sayuni na wale waliobakia Yerusalemu
wataitwa watakatifu, yeyeto aliyeandikwa chini anaishi Yerusalemu. [4] Hii itatokea
pale ambapo Bwana atasafisha uchafu wa mabinti wa Sayuni, na atasafisha madoa
ya damu kutoka kati ya Yerusalemu, kwa namna ya roho ya hukumu na roho ya
kuungua na moto. [5] Tena juu ya mlima wote wa Sayuni na mahali pakuksanyikia,
Yahwe atafanya wingu na moshi kwa wakati wa mchana na moto unaong'a wakati
wa usiku; na itakuwa dari juu ya utukufu wote. [6] kutakuwa na kivuli kwenye makazi
wakati mchana kuzuia jua, na kimbilio na mfuniko kutoka kwenye mawimbi na
mvua.

# 5

[1] Acha niimbe kwa mpendwa wangu mzuri, wimbo wa mpendwa wangu kuhusu
shamba la mzabibu. Mpendwa wangu ana shamba kwenye mlima wenye rutuba.

2 Analilima, anaondoa mawe, na anaotesha aina ya mizabibu iliyo bora. Na hujenga
mnara katikati ya shamba akichimba shinkizo ndani yake. Anasubiria mzabibu uzae
matunda lakini unazaa zabibu mwitu. 3 Kwa hiyo sasa, wakazi wa Yerusalemu na
watu wa Yuda, toa hukumu kati yangu na shamba la mzabibu. 4 Je ni kitu gani cha
ziada unaweza ukakifanya kwenye shamba langu la mizabibu, ambacho sijakifanya?
ninapotamzamia izae matunda, kwa nini inazaa matunda mwitu? 5 Sasa nitawambia
kitu nitakacho kifanya kwenye shamba langu la mzabibu: nitaondoa uzio, nitaligeuza
kuwa malisho, Nitavunja ukuta wake chini. Na itakanyagwa chini. 6 Nami
nitaliharibu wala halitapaliliwa wala kuilmwa, bali litatoa mbigiri na miba; nami
nitayaamuru mawingu yasinyeshee mvua juu yake. 7 Maana shamba la mzabibu
la Yahwe Bwana wa majeshi ni nyumba ya Israeli, na mtu wa Yuda ndio mazao
yake ya kupendeza; anaisubiria haki lakini badala ya yaki kuna mauwaji; maana
haki, lakini badala yake ni kelele zikihitaji msaada. 8 Ole wao wanaoungana nyumba
kwa nyumba, shamba kwa shamba, mpaka wanamaliza, na umebaki mwenyewe
kwenye shamba! 9 Yahwe wa majeshi ameniambia mimi, nyumba nyingi zitakuwa
wazi, hata kubwa na zinazovutia, hakuna mwenyeji yeyote. 10 Maana mashamba ya
mizabibu la nira kumi lilitoa bathi moja tu, na homeri ya mbegu itatoa efa tu. 11 Ole
wao wanaoamka asubuhi na mapema kutafuta pombe kali, wale wanaokaa usiku
wa manane mpaka pombe inawaka moto. 12 Wanasherekea kwa kinubi, kinanda,
kigoma, filimbi, na mvinyo, lakini hawazitambui kazi za Yahwe, wala hawaziangalii
kazi za mikono yake. 13 Kwa hiyo watu wangu wameenda kifungoni kwa kukosa
uelewa; viongozi wao wakuheshimiwa wanashinda na njaa, na watu wao hana kitu
cha kunjwa. 14 Hivyo basi kuzimu kumeongeza ladha yake na imefungua kinywa
chake kwa kiasi kikubwa; wasomi wao, viongozi wao, manabii na wenye furaha
miongoni mwao, watashuka kuzimu. 15 Mtu atalazimishwa kuinama chini, na watu
watakuwa wayenyekevu; na macho yao ya kujivuna yatatupwa chini, 16 Yahwe
wa majeshi atainuliwa katika haki yake, na Mungu mtakatifu atajidhirisha kuwa
mtakatifu kwa haki yake. 17 Ndipo kondoo watalishwa kama wako kwenye malisho
yao wenyewe, na katika uharibifu, kondoo watachungwa kama wageni. 18 Ole wao
wanaovuta pamoja na waovu kwa kamba isiyo na maana na wanaovuta pamoja na
dhambi kwa kamba za gari. 19 Ole kwa wale wasemao, '' Basi na Mungu afanye
haraka, basi afanya upesi, ili tuweze kuona kinachotokea; na tuache mipango ya
Mtakatifu wa Israeli ije, ili tuifahamu.'' 20 Ole wao waitao uovu wema, na wema
ni uovu; inayowakilisha giza kama mwanga, na mwanga kama giza; inayowakilisha
kitu kichungu kama kitamu, na kitamu kama kichungu! 21 Ole kwa wale wenye
busara machoni mwao, na buasra kwa uelewa wao! 22 Ole wao ambao ni washindi
kwa kunjwa mvinyo, na wazoefu wa kuchanganya pombe kali; 23 ambao wako huru
kumpa haki mtenda maovu, na kuwanyima haki wenye haki! 24 Hivyo basi kama
ndimi za moto zinazokula mabua, kama majani makavu yanavyochomwa na moto,
hivyo basi mizizi yake itaoza na maua yake yataperuka kama mavumbi. Hii itatokea
kwa sababu wameikataa sheria ya Yahwe wa majeshi, na kwa sababu wamedharau
neno la Mtakatifu wa Israeli. 25 Hivyo basi hasira ya Yahwe imewaka juu ya watu
wake. Ameunyoosh mkono wake juu yao na kuwaadhibu wao. Milima inatikisika,
na maiti ni kama takata mitaani. Katika mambo yote haya, hasira yake haijapungua;
badala yake, ameonyoosha mkono wake nje. 26 Atapandisha bendera ya ishara mabali
na mataifa na atapuliza filimbi kwa wale walio mwisho wa nchi. Tazama watakuja
wakikimbia mara moja. 27 Hakuna tairi wala mashaka miongoni mwao; hakuna
asinzae wala kulala usingizi. Au kama mkanda uliolegea, wala kamba za viatu
kukatika. 28 Mishale yao ni mikali na upinde wao umejikunja; kwato za farasi wao' ni
kama jiwe, na gari lao magurudumu yake ni kama miba. 29 Mngurumo wao utakuwa

kama wa simba, wataunguruma kama mtoto wa simba. Watanguruma na kukamata
mawindo na kuvuta mbali, na hakuna hatakayeokolewa. [30] Siku hiyo ataunguruma
juu ya mawindo kama vile bahari kwa kishindo. Yeyote atakayeangalia nchi, ataona
giza na mateso; hata mwanga hutafanjwa kuwa mweusi kwa mawingu.

# 6

[1] Nyakati zile za kifo cha mfalme Uzzia, nilimuona Bwana akiketi katika kiti
cha cha enzi; alikuw juu na mahali palipo inuka, na pindo la vazi lake limejaa
hekaluni. [2] Juu yake kuna maserafi; kila moja lina mabwa sita; mawili yamefunika
uso wake, na mawili yamefunika miguu yake, na mawili ya kurukia. [3] Kila mmoja
anaitana na mwenzake nakusema, ''Mtakakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu. ni Yahwe wa
majeshi! Dunia yote imejaa utukufu wake.'' [4] Misingi ya vizingiti imeshtuka kwa
sauti ya mtu aliye nje, na njumba imejaa moshi. [5] Ndipo nikasema,'' Ole wangu''
ninastahili adhabu maan mimi ni mtu mwenye midomo michafu, na ninaishi na
watu wenye midomo michafu, maana macho yangu yamemuona Mfalme, Yahwe,
Yahwe wa majeshi.'' [6] Ndipo mmoja wa maserafi akaruka juu yangu; mkononi
mwake akiwa amebeba makaa ya mawe yanayong'aa, ameyachukuwa kwa koleo
mathebauni. [7] Akaugusa mdomo wangu kwa makaa ya mawe na akasema, ''Ona,
makaa ya mawe yameshika midomo yako; maovu yako yameondolewa, na dhambi
zako zimelipiwa kwa hili.'' [8] Nilisikia sauti ya Bwana ikisema, Nimtume nani; nani
ataenda kwa niaba yetu?'' Ndipo nikasema, Niko hapa; nitume mimi.'' [9] Akasema
nenda na uwambie watu, ' mnasikiliza lakini hamelewi; anaona lakini hamuangalii.
' [10] Nenda ufanye mioyo ya watu hawa kuwa migumu, na masikio yao kuwa mazito,
na macho yao kuwa vipofu. Hivyo basi wanaweza kuona kwa macho yao, kusikia
kwa masikioa yao, na kuelewa kwa mioyo yao wakajeuka na kuponjwa. [11] Ndipo
nikasema, ''Bwana, mda gani?'' Akanijibu, mpaka mji itakapopata ajali na kuharibiwa
na pasipo wakazi, na nyumba hazina watu, na nchi imeanguka katika ukiwa mtupu,
[12] na mpaka pale Yahwe atakapo wapeleka watu mbali, na upweke wa nchi ni
mkubwa. [13] Hata kama makumi ya watu watabaki kwenye nchi, itaharibiwa kwa
mara nyingine kama mwaloni uliokatwa chini na shina lake likabaki, mbegu takatifu
kwenye kisiki chake.''

# 7

[1] Siku zile wakati Ahazi mtoto wa Yothani mtoto wa Uzia, mfalme wa Yuda, Rezeni
mfalme wa Amramu, na Peka mtoto wa Remaelia, mfalme wa Israeli, walienda
Yerusalemu kupigana vita nao, lakini hawakuweza kushinda vita. [2] Ilitaarifiwa
kwa nyumba ya Daudi kwamba Amramu amejiunga na Efraimu. Moyo wake na
moyo watu wake ukatetemeka, kama vile miti ya misitu inavyopepea kwa upepo.
[3] Ndipo Yahwe akamwambia Isaya, ''Nenda nje na kijana wako, Sheari Jashubu
ukaonane na Ahazi mwisho wa mfereji wa birika la juu, katika njia kuu ya uwanja
Dobi. [4] Mwambie, 'awe makini, awe mtulivu, asiogope au vitisho kwa sababu
ya mikia hii miwili ya vingi hivi vitokavyo moshi, kwa sababu ya hasira kubwa
ya Resini na Amramu, na mtoto wa Remalia. [5] Amramu, Ephraimu, na mtoto
wa Remaeli wamepanga mabaya juu yako; wamesema, '' njooni tuwavamie Yuda
na kuwaogopesha, [6] njooni tujipange na tumueweke mfalme wetu ndani ya Yuda,
mtoto wa Tabaeli.'' [7] Bwana Yahwe asema, ''haitatokea; haitaonekana, [8] maana
kichwa cha Amramu ni Damaskasi, na kishwa cha Damaskasi ni Rezini. Ndani
ya miaka sitini na tano, ndoto za Ephraimu zitasambaratishwa na hapatakuwa
na watu. [9] Efraimu ni kichwa Samaria, na kishwa cha Samaria ni mtoto wa
Remaria. Na kama hamtasimama imara katika imani yenu, hakika hamtakuwa
salama''. [10] Bwana akaongea tena na Ahazi, [11] ''Omba ishara ya Yahwe Mungu

wako; omba juu ya hilo kwa kina au kwa kiwango cha juu." 12 Lakini Ahazi
anasema, sintomba wala kumjaribu Yahwe." 13 Hivyo Isaya akajibu, "sikilizen,
nyumba ya Daudi. Je haijatosha kwa watu kuujaribu uvumilivu wa watu? Je ni
lazima kuujaribu uvumilivu wa Mungu? 14 Hivyo basi Mungu mwenyewe atawapa
yeye mwenywe ishara: ona, mwanamke bikira atapata mimba na kumzaa mtoto, na
atamwita Emanueli. 15 Atakula siagi na asali na wakati anapojua kuyakataa maovu
na kuchagua mema. 16 Maana kabla mtoto ajajua kuyakataa maovu na kuchagua
mema, nchi ambayo wewe unawachukia wafalme itakuwa ukiwa. 17 Yahwe ataleta
juu yako, juu ya watu wako, na juu ya nyumba ya baba yako siku hazijatimmia tangu
Efraimu alipompokea Yuda- atamleta mfalme wa Asiria." 18 Mda huo Yahwe atapuliza
filimbikwa ajili ya kupaa kutoka mkondo wa umbali wa Misri, na maana nyuki kutoka
nchi ya Asiria. 19 Zitakuja na kukaa chini ya korongo, ndani ya mapango ya miamba,
kwenye vichaka vya miba, na kwenye malisho. 20 Katika mda huo Bwana atamnyoa
kichwani kichwani na nywele za miguuni kwa wembe ulioazimwa mto Efrarate—
mfalme wa Asiria - na vilevile utasafisha ndevu zote. 21 Siku hiyo, mtu atahifadhi
ndama na na kondoo wawili, 22 na kwasababu ya maziwa yatakayo patikana ni mengi,
atakula siagi, maana kila atakaye bakia kwnye nchi atakula siagi na asali. 23 Mda huo,
kutakuwa na maelfu ya mizabibu na thamani elfu za shekeli, hakutakuwa na kitu
zaidi ya kuzalisha mbigiri na miiba. 24 Watu watenda pale kuwinda kwa upinde, kwa
sababu nchi yote itazalisha mbigiri na miiba. 25 Watakaa mbali na vilima vitalimwa
kwa jembe, kwa sababu ya hofu ya mbigiri na miiba, lakini hapo patakuwa mahali
pa kuchungia ngo'mbe na kondoo

# 8

1 Yahwe ameniambia mimi, " chukua meza kubwa na uandike juu yake, 'Maheri
Shalal Hash Baz.' 2 Nitachagua mashahidi waaminifu wanishuhudie mimi, kuhani
Uria, Zakaria mototo wa Yeberekia." 3 Nilienda kwa huyo nabii mwanamke alipata
mimba na kumzaa mtoto. Halafu Yahwe akaniambia, "Muite jina lake Shalal Hash
Baz; 4 Maana kabla mtoto ajajua kulia, 'Baba yangu, 'Mama yangu; utajiri wa
Damaskasi, na mateka wa Samaria watachuliwa na mfalme wa Asiria. 5 Yahwe
aliongea na mimi tena, 6 Kwa sababu watu hawa wameyakataa maji ya Shiloa
na ni furaha kwa Rezeni na mtoto wa Remalia, 7 Hivyo basi Bwana anakairbia
kuwaletea maji maji ya mto, yenye nguvu na mengi, mfalme Asiria na utukufu
wake utakuja juu na kupita juu ya mifereji yake atafurika juu ya kingo zote. 8 Mto
utafurika kuelekea Yuda, utafurika mpaka kufika kwenye shingo yako. Mabawa
yake yaliyonyooshwa utajaza upana wa nchi, Emanueli." 9 Nyie watu mtavunjika
vipande vipande, Sikilizeni, nyote muishio nchi zilizo mbali; jiandaeni wenyewe
na mtavunyika vipande vipande. 10 utatengeneza mpango, lakini haufanyiwa kazi;
maana Mungu yuko pamoja nasi. 11 Yahwe ameiniambia mimi, kwa mkono wake
imara juu yangu, na amenikataza nisitembee katika njia za watu hawa. Nisiseme,
12 Ni fitina habari ya mambo ambayo watu hawatasema, ni fitina msihofu wala
msiogope. 13 Yahwe wa majeshi ambaye mtakaye muheshimu kama mtakatifu; yeye
ndie mtakayemuogopa na yeye ndiye mtakayemuhofia. 14 mtakatifu; lakinia takuwa
kama jiwe la kikwazo na mwamba wa kujikwaza kwa nyumba zote za Israeli. Na
atakuwa mtego na mtego kwa watu wake Yerusalemu. 15 Wengi watajikwaa juu
yao na kuanguka na kuvunjika, na kutekwa na kukamata mateka. 16 Ufunge huo
ushuhuda, tia muhuri, na uwape wafuasi wangu, 17 Nitamsubiri Yahwe, afichaye uso
wake kutoka nyumba ya Yakobo; Nitamsubiri yeye. 18 Ona, Mimi na watoto ambaye
Yahwe amenipa mimi ni ishara na maajabu tu katika Israeli kutoka kwa Yahwe
wa Majeshi yeye aishiye mlima wa Sayuni. 19 Watakuambia wewe, "tafuta habari

kwa watu wenye pepo na wachawi'', walio kama ndege na kunong'ona dua. Lakini
hawataacha kutafuta habari kwa Mungu wao? Je waenende kwa watu waliokufa
badala ya walio hai? [20] Kwa sheria na kwa ushuhuda! kama hawatayasema mambo
hayo ni kwa sababu hakuna mwanga wa alfajiri. [21] Nawatapita katikati ya nchi kwa
shida kubwa na njaa. Walipokuwa na njaa, walipatwa na hasira na kumlaani mfalme
wao na Mungu wao, na wakajeuza macho yao juu. [22] Wataiangalia nchi na kuona
dhiki, giza, na ukandamizaji wa viza. Watapelekwa kwenye nchi ya giza.

# 9

[1] Viza itaondolewa kwa yeyote ambaye yuko kwenye dhiki. Katika kipindi cha
awali aliifedhehesha nchi ya Zebuluni na nchi ya Naftali, lakini kipindi cha baadae
ataifanya itukuke, njia ya kuelekea baharini, mbele ya Yordani na mataifa ya Galilaya.
[2] Watu wanotembeakatika giza wameona wameona mwanga mkubwa; wale waishio
katika nchi ya uvuli wa mauti, mwanga umewaka juu yao. [3] Umeliongeza taifa;
umeongeza furaha yao. Wamefurahia mbele yako kama furaha ya kipindi cha
mavuno, kama watu wanavyofurahi kugawanya nyara. [4] Maana nira ya mzigo
wake, boriti katika mabega yake, fimbo ya mkandamizaji, umesambaratisha ndoto
kama siku ya Midiamu. [5] Kila buti likanyagalo gasia na vazi limekwisha kwenye
damu itachomwa, mafuta kwa moto. [6] Kwetu mtoto amezaliwa, kwetu mtoto
ametoka; na mtawala atakuwa kwenye mabega yake; na jina lake ataitwa mshauri
wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa Amani. [7] Enzi yake
na amani yake haitakuwa na mwisho, maana anatawala katika kiti cha enzi cha
Daudi, na juu ya ufalme wake, ataanzisha hukumu ya haki, tangu sasa na hata
milele. Bidii ya Yahwenwa majeshi itafanya haya. [8] Bwana alituma neno juu
ya Yakobo, na ikaanguka juu ya Israeli, [9] Watu wote watajua, Hata Samaria na
wakazi wote wa Samaria, wanaongea kwa kiburi na moyo wenye kiburi, [10] Matofali
yameanguka, lakini tutajenga tena kwa jiwe la patasi; mkuyu umekatwa chini,
lakini tutaotesha mierezi katika eneo lao. [11] Hivyo basi Yahwe atamwinua juu yao
Rezini, adui zake, atawakoroga adui zake, [12] Waaramea upande wa mashariki, na
wafilisti upande wa magharibi. Nao watamla Israeli kwa mdomo uliowazi. katika
mambo yote haya hasira yake haijapungua; badala yake ameunyosha mkono wake
nje. [13] Lakini hawatageuka kwa yule anayewapiga wao, wala kumtafuta Yahwe wa
majeshi. [14] Hivyo basi yao atakata kichwa nakiwiwili cha Israeli, kuti na nyasi,
katika siku moja. [15] Viongozi na watu wenye vyeo na manabii wanaofundisha kuwa
uongo ni mkia. [16] Wale wanaowaongoza watu hawa wanawaongoza vibaya, na
wale wanaongozwa wameangamia. [17] Hivyo basi Bwana atafurahia juu ya vijana
wadogo wala hatakuwa na huruma kwa yatima na wajane, maana kila mmoja hana
Mungu na ni watenda dhambi, na kila mdomo unazungumza matendo mabaya.
Mambo yote haya, hasira yake haijapungua; badala yake mkono wake umenyooka
hata sasa. [18] Matendo mabaya yataungua kama moto, moto hulao mbigili na
miiba; itachoma hata vichaka vya mwitu, na safu ya moshi mkubwa upaa. [19] Japo
hasira ya Yahwe wa majeshi imeunguza, na watu ni kama mafuta kwenye moto.
Hakuna mtu aliyemuacha ndugu yake. [20] Watanyakuwa chakula katika mkono
kulia lakini bado watasikia njaa; watakula chakula kwa mkono wa kushoto lakini
hawataridhika. Kila mmoja atakula nyama ya mkono wake mwenyewe. [21] Manase;
kwa pamoja watavamia Yuda. Mambo yote haya, hasira yake haitapungua; badala
yake, amenyoosha mkono wake hata sasa.

# 10

[1] Ole wao watimizao sheria zisizo za haki na waandikao sheria zisizo na haki.

2 Wanawanyima wahitaji haki yao, wanawaibia watu wangu walio masikini haki zao,
wajane mateka wao, na kuwafanya waliofiwa na baba zao mawindo yao! 3 Hutafanya
nini siku ya hukumu pale siku ya uaribifu itakapokuja kutoka mbali, utakimbilia
msaada kwa nani? na utauacha utajiri wako wapi? 4 Hakuna kitakachobaki, utaota
miongoni mwa wafungwa au kuanguka miongoni mwa wauwaji. Katika mambo yote
haya, hasira yake haijapungua; badala yake mkono wake ameunjoosha hata sasa.
5 Ole kwa watu wa Asiria klabu ya asira yangu, fimbo ya asira yangu! 6 Nimemtuma
juu ya taifa lenye kiburi na juu ya watu waliobeba uwingi wa hasira. Ninaamuru
chukua nyara, chukua mawindo, na kuwakanyaga wao kama matope mitaani.
7 Lakini hichi sicho alichomaanisha, wala sivyo afikiriavyo. Maana katika moyo wake
ni kuharibu na kuondoa mataifa. 8 Maana amesema, '' wakuu wote sio wafalme?
9 Je? kalno si kama Karkemish? Je Hamathi si kama Arpadi? Je Samaria si kama
Demeski? 10 Kama mikono yangu imeshinda falme za ibada ya sanamu, ikiwa sanamu
zao za kuchonga ni bora kuliko sanamu za Yerusalemu 11 na Kama nilivyofanya kule
Samaria na sanamu zake zisizo na maana, je sitaweza kufanya hivyo Yerusalemu
na sanamu zake?'' 12 Pindi ambapo Bwana alipoimaliza kazi kwenye mlima Sayuni
na juu ya Yerusalemu, nitayaadhibu maneno ya moyo wenye kiburi ya mfalme wa
Asiria na majivuno yake. 13 Kwa maana amesema, ''Kwa nguvu zangu na kwa hekima
yangu niliyoifanya. na Nimeelewa, na nimeondoa mipaka ya watu. nimewaibia
akiba yao, ni kama nilioileta chini kwa wenyeji wake. 14 Na mkono wangu umezitoa
mali za mataifa kama vile mtu ayakusanyavyo mayai, kama nilivyokusanya dunia
yote. Hakuna atakayeperusha mabawa yake au kufungua midomo yake au kulia.''
15 Je shoka lijisifu lenyewe juu ya mtu anayelitumia? Je litajisifia lenyewe zaidi ya
yule anaelitumia kukatia? Au fimbo imuinuae yeye ambaye si mti. 16 Hivyo basi
Yahwe wa majeshi atatuma wadhaifu miongoni mwa wasomi wa kijeshi; na chini
ya utukufu na kuteketea kama kuteketea kwa moto. 17 Mwanga wa Isreli utakuwa
moto, na Mtakatifu wake atakuwa ni moto unaoteketeza na kula mbigiri siku moja.
18 Yahwe atauteketeza utukufu wa msitu wake na shamba lake linalostawi, vyote nafsi
na mwili; itakuwa kama vile mgonjwa apotezae maisha yake. 19 Mabaka ya miti ya
misitu itakuwa michache sana, ambayo mtoto anaweza kuyahesabu. 20 Siku hiyo,
mabaki ya Israeli, familia ya Yakobo ambayo imekimbia, hawatategemea kushindwa,
lakini watamtegemea Yahwe, Mtakatifu wa Israeli. 21 Mabaki ya Yakobo yatarudi
kwa Mungu mwenye nguvu. 22 Kwa kupitia watu wako, Israeli ni kama mchanga
kama pwani ya bahari, Mabaki yao tu ndio yatakayorudi. Uaribifu wa amri, na
mahitaji ya wingi wa haki. 23 Maana Bwana wa majeshi, anakaribia kuleta uharibifu
utachukua nafasi kubwa kitika nchi. 24 Hivyo basi Bwana Yahwe wa majeshi
anasema, ''watu wangu mhishio Sayuni, msiwaogope watu wa Asiria. Atawangamiza
nyie kwa fimbo na atawanyua wafanyakazi juu yenu, kama ilivyotokea kwa Wamisri.
25 Msimuogope, kwa mda mfupi hasira yangu itakwisha juu yenu, na hasira yangu
italeta uharibifu.'' 26 Hivyo Yahwe wa majeshi atapiga mjeledi juu yenu kama vile
alivyoishinda Midiani karibu na mwamba Orebu. Na atanyanyua fimbo yake juu ya
bahari kama alivyofanya kule Misri. 27 Siku hiyo mzigo wake utanyanyuliwa kwenye
mabeba yako na nira katika shingo yako, nayo nira itaharibiwa kwa sababu ya unene.
28 Adui amekuja Aiathi na amepitia Migroni; katika Michmashi ameyahifadhi mahitaji
yake. 29 Wamevuka juu ya njia na wamepunzika huko Geba. Rama inatetemeka na
Gibea ya Sauli imekimbia. 30 Lia kwa sauti, ewe binti wa Galimu! sikiliza, Laishashi!
Maskini Anathothi! 31 Madmena ni mkimbizi na mkazi wa Gebuni wamejikusanya
wanakimbia kutafuta msada. 32 Siku hizi za leo atasimulia huko Nobi na atatingisha
mlima wa binti Sayuni, mlima wa Yerusalemu. 33 Tazama, Bwana Yahwe wa majeshi
atapunguza matawi kwa nguvu za kutisha; miti mirefu itakatwa chini, wanaojivuna

wataangushwa. 34 Atang'oa vichaka vya msitu kwa shoka, Lebanoni na utukufu wake
utaanguka.

## 11

1 Miti itachipukia katika mizizi ya Yese, na matawi yanayotokana na mizizi
yatazaa matunda. 2 Na roho wa Bwana atashuka juu yake, roho wa hekima na
maelewano, roho ya maelekezo na ukuu, roho ya maarifa na hofu ya Yahwe. 3 Furaha
yake itakuwa hofu ya Bwana; hatatoa hukumu kwa kile anachokiona, wala atatoa
maamuzi kwa kile anachokisikia. 4 Badala yake atawahukumu masikini kwa haki na
atafanya maamuzi kwa usawa na unyenyekevu. Ataamurisha mgomo wa dunia kwa
fimbo ya mdomo wake, na punzi ya midomo yake, atawauwa waovu. 5 Haki itakuwa
mkanda wa viuno kiuno chake kuzunguka mapaja yake. 6 Mbwa mwitu atakaa
pamoja na kondoo, na chui watalala chini pamoja na mtoto wa mbuzi, ndama, mtoto
wa simba na ndama pamoja na ndama aliyenona. Mtoto mdogo atawaongoza wao.
7 Ng'ombe na dubu watachungwa pamoja. Na watoto wao watalala pamoja. Simba
atakula majani kama ng'ombe. 8 Mtoto atacheza juu ya chimo la nyoka, na mtoto
aliyeachwa ataweka mkono wake katika pango la nyoka. 9 Hawataumizwa wala
kuharibiwa kwenye mlima mtakatifu; kwa maana dunia itakuwa imejaa maarifa ya
Yahwe, kama maji yajaavyo kwenye bahari. 10 Siku hiyo mzizi wa Yese utasimama
kama bendera ya watu. Taifa litamtafuta yeye nje, na mahali pake pakupumzikia
patatukuka. 11 Siku hiyo, Bwana ataunyoosha mkono wake tena kuokoa mabaki ya
watu wake yaliyosalia huko Asiria, Misri, Pathrosi, Kushi, Shinari, Hamathi, na kisiwa
cha bahari. 12 Ataweka bendera kwa kwa mataifa na atakusanya Waisrel waliotupwa
na watu wa Juuda waliotawanyika kitika pembe nne za dunia. 13 Ataujeuza wivu wa
Efraimu, na ukatili wa Yuda utakomeshwa. Efraimu atamuonea wivu Yuda, Yuda
hatakuwa adui wa Efraimu tena. 14 Badala yake, watashuka chini kwenye mlima
wa Wafilisti upande wa magharibi, na pamoja watateka watu mashariki. Watavamia
Edomu na Moabu, na watu wa Amoni watawatii wao. 15 Yahwe atauharibu kabisa
ghuba ya bahari ya Misri. Kwa mawimbi makali ambayo yanavuma juu ya mtoto
Efurate na itagawanyika katika mifereji saba, hivyo unaweza ukapita juu kwa viatu.
16 Kutakuwa na njia kuu kwa ajili ya mabaki ya watu kurudi kutoka Asiria, maana
kuna Waisraeli wanaokuja kutoka nchi ya Misri.

## 12

1 Siku hiyo utasema, "Nitakushukuru wewe, Yahwe. Japo ulikuwa na hasira na
mimi, laana yako imeondoka mbali, na umenifariji mimi, 2 Ona Bwana ni wokovu
wangu; nitamwamini na sitakuwa na hofu, kwa Yahwe, ndio, Yahwe ni nguvu yangu
na wimbo wangu. Amekuwa wokovu wangu." 3 Kwa furaha utachota maji kwenye
kisima cha wokovu. 4 Siku hiyo utasema, "Mshukuru Yahwe na ita jina lake; tangaza
matendo yake miongoni mwa watu, tangaza jina lake limeinuliwa. 5 Mwiimbie
Yahwe, maana ametenda matendo yaliotukuka; acha hili lijulikane dunia nzima. 6 Lia
kwa nguvu na piga kelele kwa furaha, enyi wakazi wa Sayuni, maana katikati yenu
ni mtakatifu wa Israeli.

## 13

1 Tamko kuhusu Babeli, ambalo Isaya mtoto wa Amozi alipokea: 2 Kwenye mlima
wa wazi imewekwa bendera ya ishara, lia kwa sauti kwao, wapungie mikono waende
kwenye lango la wenye vyeo. 3 Nimewamuru watakatifu wangu, ndio, nimewaita
watu wangu wenye nguvu kutekeleza asira yangu, na hata watu wangu wanojigmba
na kujiinua wenyewe. 4 Kelele za umati wa watu kwenye milima, za watu wengi!
Kelele za ghasiaza ufalme kama mataifa mengi yamekusanyika pamoja! Yahwe

wa majeshi anapanga jeshi kwa vita. 5 Wametoka katika nchi ya mbali, kutoka
juu ya upeo wa macho. Ni Yahwe na silaha zake za hukumu, kuhiharibu nchi
yetu. 6 Omboleza maana siku ya Yahwe imekaribia; itakuja na uharibifu kutoka
kwa Mwenyenzi. 7 Hivyo basi mikono ining'inizwe kama kiwete, na kila moyo
ulioyeyuka. 8 Itawatisha; maumivu na uchungu atawapa wao, kama mwanamke
ambaye anajifungua. Watangalia kwa kushangaa kwa kila mmoja mmoja; nyuso
zao zitakuwa kama moto. 9 Tazama, siku za Yahwe zinakuja na laana kali wingi
wa hasira, kuifanya nchi yenye ukiwa na kuharibu wenye dhambi katika nchi.
10 Nyota ya mbinguni na matangamano havitatoa nuru yake. Jua litakuwa giza na
hata mwenzi hautaangaza. 11 Nitaihadhibu nchi kwa maovu yake na makosa ya
uovu wao. Nitamaliza kiburi cha majivuno na nitawashusha wenye kiburi wasiwe
makali. 12 Nitawafanya watu kuwa nadra zaidi ya dhahabu nzuri na watu kuwa
vigumu kupatikana zaidi ya dhahabu safi ya Ofiri. 13 Hivyo basi nitazifanya mbingu
kutingishika, na dunia itayumba kutoka sehemu iliyoko, Kwa hasira ya Yahwe wa
majeshi, na siku ya hasira yake. 14 Kama Paa anayewindwa au kama kondoo wasio
na mchungaji, kila mtu atageukia watu wake na kukimbia kwenye nchi yake. 15 Kwa
yeyote atakayeonekana atauliwa, na yeyote atakayekamatwa atauliwa kwa upanga.
16 Watoto wao watakatwa vipandevipande mbele ya macho yao. Nyumba zao
zitavamiwa na wake zao watabakwa. 17 Tazama, ninakaribia kuwakoroga Wamede
ili wawavamie wao, ambao hawaoni maana ya fedha wala furaha ya dhahabu.
18 Mishale yao itawachoma vijana wadogo. Hakutakuwa na shimo kwa watoto wao na
hawatawacha watoto wao. 19 Na Babali ufalme unaovutia zaidi, fahari ya mapambo
ya wakaldyo, itaangamizwa na Mungu kama Sodoma na Gomora. 20 Hapatakuwa
na wenyeji wala wakazi kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Mwarabu atapiga
hema lake uko wala wachungaji hawatalaza mifugo yao pale. 21 Lakini wanyama
pori wa jangwani watalala pale. Nyumba zao zitajaa bundi; na mbuni watakaa huko
na mbuzi pori wataruka pale. 22 Fisi watalia kwenye ngome yao, na mbeha katika
maeneo yao mazuri. Mda wao umekaribia, na siku zao hazitachelewa.

# 14

1 Yahwe atakuwa na huruma juu ya Yakobo; atamchagua tena Israeli na kumrud-
isha tena kwenye nchi yake. Wageni wataungana nao na wataambatana wenyewe na
nyumba ya Yakobo. 2 Mataifa yataletwa katika maeneo yao wenyewe. Ndipo nyumba
ya Israeli itawachukwa katika nchi ya Yahwe kwa watumishi wa kiume na wakike.
Watachukuwa wafungwa wale waliokamatwa, na watawaongoza wale waliokuwa
wanawanyanyasa. 3 Siku hiyo Yahwe atatoa pumziko kutoka kwenye mateso na
maumivu, na kutoka kwenye kazi ngumu ambayo waliitajika kuzifanya, 4 mtaimba
hii kauli wimbo juu ya mfalme wa Babeli, "Ni kwa jinsi gani wayanyasaji wamefika
mwisho, kiburi cha hasira kimekwisha! 5 Yahwe amevunja wafanyakazi waovu,
fimbo ya hao viongozi, 6 inayowapeleka watu kwenye laana na mapigo yasiyopimika,
wanoongoza taifa kwa hasira,. 7 yote iko katika punziko na utulivu; wmeanza
kusherekea kwa kiimba. 8 Hata mti wa mseprasi inafuhaia pamoja mierezi ya
Lebanoni; inasema, Tangu ulipoweka chini, hakuna mkata kuni aliyekuja kutungusha
sisi, 9 Kuzimu haina hamu kwa ajili yako unaye enda pale. Watafufuka waliokufa
kwa ajili yako, wafalme wote wa dunia, wafanje watoke katika viti vyao vya enzi,
wafalme wote wa mataifa. 10 Watazungumza na kukuambia wewe, 'umekuwa dhaifu
kama sisi. 11 Kiburi chako kimeshushwa kuzimu na sauti kifaa cha kamba yako.
Buu wameongezeka chini yako na vijidudu vinakufunika wewe.' 12 Kwa jinsi gani
ulivyoanguka kutoka mbinguni, nyota ya siku, jua la asubuhi! ni kwa jinsi gani
mlivyoshushwa chini, umeyashinda mataifa! 13 Unasema katika moyo wako, ' Nitapaa

kutoka juu mbinguni, nitanyanyua enzi yangu juu ya nyota za Mungu, na nitakaa
kwenye mlima wa kukusanyikia, kwa mbali kufika kaskazini. 14 Nitapaa juu umbali
wa mawingu; Nitalifanya mimi mwenyewe kama Mungu aliye juu zaidi.' 15 Lakini
kwa sasa umeshushwa chini kuzimu, kwenye kina cha shimo. 16 Wale wanaokuona
watakuangalia wewe, watakuangalia sana. Watasema, Je ni huyu mtu aliyefanya
dunia itetemeke, nani aliyetingisha falme, 17 ni nani aliyefanya dunia kama jangwa,
ni nani aliyeharibu miji yake, na hataki kuwachia wafungwa waende nyumbani?'
18 Wafalme wote wamataifa, wote kwa pamoja wamelala chini kwa heshima, kila
mtu kwa kaburi lake. 19 Lakini umetupwa nje ya kaburi lako kama tawi lilivyotupwa
mbali. Maiti imekufunika kama vazi, na wale wanaochomwa kwa upanga, nani wale
washukao mpaka misingi ya shimo. 20 Hautaunganishwa pamoja katika mazishi, kwa
sababu umeiharibu nchi yako na kuuwa watu wako. Watoto wa watenda maovu
hawatatajwa tena.'' 21 Anda machinjio kwa ajili ya watoto wake, kwa sababu ya
uovu wa mababu zao, hivyo basi hawatanyanyuka juu na na kuimiliki aridhi ya
nchi iliyojaa miji ya dunia yote.'' 22 Nitapanda juu yao''- hili ni tamko la Yahwe wa
majeshi. Nitang'oa jina katika Babeli, uzao, na ukoo''- hili ndilo tamko la Yahwe.
23 Tena nitaifanya nchi hiyo kuwa makao ya bundi, dimbwi la maji, nanitawafagia
kwa mfagio wa uharibifu''- hili ni tamko la Yahwe wa majeshi. 24 Yahwe wa majeshi
ameapa, ''Hakika, kama nilivyodhamiria, itakuwa kama ilivyo; na kama nilivyo
kusudia itakuwa: 25 Nitawavunja Waasiria kwa mikono yangu, na kukanyaga milima
kwa miguu yangu mwenyewe. Hivyo nira yake itanyanyuliwa juu yao na mzigo
juu ya mabega yao.'' 26 Huu ni mpango uliokusudiwa katika nchi yote, na huu
ndio mkono ulionyanyuliwa juu ya mataifa. 27 Kwa maana Yahwe wa majeshi
amepanga hivi; ni nani atakayemzia yeye? Mkono wake umenyanyuliwa juu, ni nani
atakajemrudisha nyuma? 28 Katika miaka ambayo mfalme Ahazi alipokufa, hili ndio
tamko lilokuja: 29 Msishangilie, enyi wafilisti wote, kwamba fimbo ya kukupigia wewe
imevunjika. Maana katika njia ya nyoka atatoka fira, na watoto wake watakuwa
moto nyoka wanaopaa. 30 Na mtoto wa kwanza wa maskini watachunga kondoo wao
kwenye malisho yangu, na wahitaji watalala chini salama. Nitaiuwa mizizi yenu
kwa njaa ambayo atawauwa wakazi wenu wote. 31 Omboleza, ewe lang, lia, ewe mji;
ninyi nyote mtayeyukia mbali, Ufilisti. Maana kutoka kaskazini limetoka wingu la
moshi, na hakuna hata mmoja atakaye odoka kwenye nafasi yake. 32 Ni kivipi mtu
mmoja atamjibu mjumbe wa taifa? Kwamba Yahwe ameipata Sayuni, na ndani yake
walionewa watatafuta kimbilio.

# 15

1 Tamko kuhusu Moabu, Kweli, kwa usiku mmoja Ari ya Moabu imeharibiwa
kabisa na kuangamizwa; kweli, kwa usiku mmoja Kira ya Moabu itaharibiwa na
kuangamizwa. 2 Wamenda juu hekaluni, watu wa Diboni wamenda juu kuomboleza;
Moabu wanaomboleza juu ya Nebo na juu ya madeba. Vichwa vyao vimenyolewa
viko wazi na na ndevu zao zimenyolewa. 3 Wamevaa nguo za magunia katka mitaa
yao; juu ya dari zao na kila kona ya mitaa yao, kuyeyuka kwa kumwaga machozi.
4 Hishiboni na Elealehi wanalia wakihitaji msaada; Sauti zao zinasikika mpaka Jahazi.
Hivyo basi vijana wa vita wa Moabu wanalia wakihitaji msaada; wanatetemeka wao
wenyewe. 5 Moyo wangu unalia juu ya Moabu; watuhumiwa wamekimbilia Zoari na
Elgathi Shelishiyahi. Wanapaa juu ya Luhithi wakilia; katika barabara ya kwenda
Horonaimu wanapiga kelele ole juu ya uharibifu. 6 Maji ya Nimrimu yamekauka;
majani yamepooza na majani yanyochikia yanakufa; hakuna ukijani hata kidogo.
7 Hivyo basi vitu vingi vimekuwa na hifadhi wameipeleka juu ya kijito maarufu.
8 Kilio kimezunguka katika himaya ya Moabu; malalamiko yamefika hata Eglaimu

na Beer-Elimu. 9 Maana maji ya Dimoni imejaa damu; Simba atawavamia wale
waliokimbia kutoka Moabu pia na walbakia katika nchi.

# 16

1 Mpeleke mwana kondoo kuongoza nchi kutoka Sela huko jangwani, kwenye
mlima wa binti Sayuni. 2 Kama ndege wazururao, viota vimetapakaa, hivyo basi
wanawake wa Moabu watavuka kwenye mto Arnoni. 3 Toa maelekezo, tekeleza
haki; toa kivuli kama usiku wakati wa mchana; wahifadhi watuhumiwa; msiwahini
watuhumiwa. 4 Waache waishi miongoni mwenu, wakimbizi kutoka Moabu; muwe
mahali pakujifichia wao wasiangamizwe.'' maana mateso yatakwisha, na uharibifu
utapungua utakuwa na kikomo, wale wanotetemeka watapotea katika nchi. 5 Kiti cha
enzi kitaanzishwa katika agano la uaminifu; na mmoja katika hema la Daudi atakaa
pale kwa uaminifu. Atahukumu kwa kufuata haki na atatenda haki. 6 Tumesikia
kiburi cha Moabu, kiburi chake, majivuno yake, na hasira yake. Lakini majivuno yake
ni maneno tu. 7 Hivyo basi Moabu atalia juu ya Moabu-wote watalia! wataomboleza,
nyie mlioharibiwa kabisa, mikate ya Kira Haresethi. 8 Shamba la Heshboni limekauka
kabisa pamoja na mizabibu ya Sibma. Kiongozi wa mataifa amekanyaga mizabibu
iliyochaguliwa na kuelekea Jazeri na kuelekea jangwani. Mizizi yake nje ya nchi;
imenda juu ya bahari. 9 Kweli nitalia pamoja Jazeri kwasababu ya shamba la
mizabibu la Sibma. Nitakuloanisha kwa machozi yangu, Heshboni, na Eleale. Maana
katika mashamba yenu kipindi cha majira ya joto matunda na mazao nitaishia
kwa kupiga kelele za furaha. 10 Furaha na shangwe zimezimwa na matunda ya
miti ya shambani; na hakuna nyimbo wala kelele katika mashamba ya mizabibu,
maana nimeweka mwisho wa kupiga kelele kwa yeyote anayetembea. 11 Hivyo,
moyo wangu unalia kama kinubi, na ndani yangu maana kwa ajili ya Kiri Hareseth.
12 Pindi ambapo Moabu wamejivika mahali pa juu, na kuingia katika hekalu kuomba,
maombi yake hayatatimiza chochote. 13 Haya ndio maneno aliyoyazungumza
Yahwe kuhusu Moabu iliyopita. 14 Tena Yahwe amesema, ''Ndani ya miaka mitatu
utukufuwa Moabu utatoweka; japo watu wake wengi, watakao bakia ni wachache,
na wasionafaida.

# 17

1 Tamko kuhusu Damaskasi. 2 Miji ya Aroera itaharibiwa. Patakuwa na nafasi kwa
ajili ya kutunzia mifugo, na hakuna hatakayeizuia. 3 Miji ilioachwa itatoweka kutoka
Efraimu, ufalme katuka Damskasi, na walobaki Aramu-watakuwa kama utukufu wa
watu wa Israeli-Hili ni tamko la Yahwe wa majeshi. 4 Itakuwa siku hiyo utukufu wa
Yakobo utapungua, utakuwa mwembamba na kunona kwa mwili wake utapungua.
5 Itakuwa kama mvuna ikusanyavyo mavuno, na mkono wake huvuna maganda ya
mazao. Itakuwa kama mtu atoae maganda ya mavuno katika bonde la Refaimu.
6 Masalia yataachwa, hata hivyo, mti wa mzabibu utatingishwa: Mizeituni miwili au
mitatu iliyo juu sana matawi yake yako juu, manne au matano katka tawi la juu katika
mti unaozaa-hili ni tamko la Yahwe, Mungu wa Israeli. 7 Siku hiyo watu watawangalia
Muumba wake, na macho yatamuangalia Mtakatifu wa Israeli. 8 Hawatangalia
madhabahu, kazi za mikono yao, wala hataangalia kile kinachofanywa na vidole
vyao, nguzo za Ashera na picha ya jua. 9 Siku hiyo miji yenye nguvu itakuwa kama
msitu uliotelekezwa na juu ya kilele cha mlima, na palipo achwa kwa sababu ya
wana wa Israeli patakuwa ukiwa. 10 Maana mmemsahau Mungu wa wakovu wenu,
na umeudharau mwamba wa nguvu zako. Hivyo basi umeotesha miti mizuri, na
mizabibu mizuri iliyotoka ugenini, 11 Siku hiyo uliootesha na fensi na kulima. Mbegu
zako zitaota mapema na kukua, lakini mavuno yatashindikana siku hiyo itakuwa

huzuni na kukata tamaa. 12 Ole! Watu wenye ghasia, Kishindo chake ni kama
mngurumo wa bahari, na kasi ya mataifa, wananguruma kama ngurumo ya maji
mengi! 13 Mataifa yataunguruma kama maji mengi yaendao kasi, lakini Mungu
atawakemea. 14 Watakimbia mbali sana na watafukuzwa kama pumba kwenye
mlima mbele ya upepo, kama mavumbi yazungukayo kwenye dhoruba. Wakati
wa usiku, ona, hofu! Na kabla ya alfajiri watakwenda; hili ndilo eneo la wale
waliotupora, na wale wanaotunyang'anya mali zetu.

# 18

1 Ole kwa nchi ya wezi wa mabawa, iliyoko mbali kupitia mito ya Ethiopia;
2 wanowatuma mabalozi wao kwa kupitia bahari, na vyombo vya majani juu ya maji.
Nendeni enyi wajumbe wepesi, kwa watu warefu na laini waishio kwenye nchi, kwa
watu wanogopa mbali na karibu, taifa lenye nguvu, wakanyagao watu, ambao mito
imegawanya nchi yao. 3 Watu wote wakaao duniani nao wakaao katika nchi, pale
ishara itakaponyanyuliwa juu ya milima, angalia; na sikilizeni mbiu itakapopulizwa.
4 Yahwe asema hivi, "nitachunguza kimyakimya kutoka nyumbani kwangu, kama
kupika joto kwenye jua, na kama ukungu kwenye joto la mavuno. 5 Kabla ya mavuno,
pale kipindi cha maua kinapoisha, na maua yako tayari kuwa zabibu. Atakata matawi
kwa kupogoa ndoano, na atakatiwa chini na kuchukua matawi yaliyotawanyika.
6 Wataachwa kwa pamoja maana ndege wa milimani na wanyama wa duniani. Ndege
watatua kwao majira ya joto, na wanyama wote watakuwa kwao kipindi cha baridi."
7 Kwa mda huo kodi italetwa kwa Yahwe wa majeshi kwa watu warefu na laini, kwa
watu wanohofia umbali na ukaribu, taifa imara na kukanyagwa chini, ambayo nchi
yao imegawanjwa na mito, Kwa sehemu ya jina la Yahwe wa majeshi, mpaka mlima
Sayuni.

# 19

1 Tamko kuhusu Misri. Ona, Yahwe atasafiri katika mawimbi mepesi na anakuja
Misri; Sanamu za Misri zitatemeka mbele yake, na mioyo ya Wamisri itayeyuka ndani
yao wenyewe. 2 Nitawachanganya Wamisri juu dhidi ya Wamisiri: Mtu atapigana
dhidi ya ndugu yake, mji dhidi ya miji, na ufalme dhidi ya ufalme. 3 Roho ya Misri
itadhohofishwa kutoka ndani. Nitauharibu ushauri wake, japo wanafikiria ushauri
wa sanamu, roho za watu waliokufa, na mizimu, na 4 Nitawacha Wamisiri kwenye
mikono ya viongozi wakatili, kiongozi imara atawaongoza wao- Hili ni tamko la
Yahwe Bwana wa majehi." 5 Maji ya bahari yatakauka juu, na mto uakauka na kuwa
mtupu. 6 Mito itakuwa michafu; mikondo ya Misri itakuwa dhii na kukauka; mwanzi
na bendera zake zitapeperushwa mbali. 7 Mianzi ya Nile, kwa mdomo wa mto Nile,
na mbegu zote zitakazo katika mashamba ya Nilezitakauka zote, zitageuka kuwa
mavumbi, na kupeperukia mbali. 8 Wavuvi watalia na kuomboleza, na wale watakao
shusha neti kwenye maji watauzunika. 9 Wafanyakazi ya kuchana kitani watafaidika
na hao washonao nguo nyeupe watajeuka kuwa mchonaji. 10 Washona nguo wa
Misri wataangamizwa; na wote waloajiriwa watahuzunika nafsini mwao. 11 Wakuu
wa Zoana ni wajinga kabisa. Washauri wenye busara wa Farao ni wapumbavu.
Unawezaje kumwambia Farao, "Mimi ni mtoto wa watu wenye busara, 12 "Wako wapi
hao watu wenye busara? mtoto wa mfalme wa zamani? Waache wakuambie? na
ijulikane kitu ambacho Yahwe wa majeshi amekipanga kuhusiana na Misri. 13 Wakuu
wa Zoani wamekuwa wajinga, wakuu wa Memphisi wamegawanyika; wameifanya
Misri iende kinyume, na mawe ya pembeni ya makabila yao. 14 Yahwe amechanganya
roho wa kuvurugwa katika yao, na wamefanya Wamisri kwenda kinyume kwa
yote wanoyafanya, kama mlevi anavyoyumbayumba uku akitapika. 15 Hakuna kitu

ambacho mtu yeyote anaweza kukifanya kwa ajili ya Misri, kama kichwa au mkia,
tawi au mwanzi. [16] Siku hiyo, Wamisri watakuwa kama wanawake. watatemeka
na kuogopa mkono wa Yahwe wa majeshi ulioinuliwa juu yao. [17] Nchi ya Yuda
itakuwa sababu ya utisho kwa Misri. Yeyote atakao wakumbusha wao kuhusu
yeye, wataogopa sana, kwa sababu ya mpango wa Yahwe, anaoukusudia juu yao.
[18] Siku hiyo kutakuwa na miji mitano katika nchi ya Misri wanaozungumza lugha
ya Kanaani na kuapa kimtii Yahwe wa majeshi. Moja kati ya miji hii itaitwa mji wa
uliohribiwa. [19] Siku hiyo kutakuwa madhabahu kwa ajili ya Yahwe katika ya nchi
ya Misri, na jiwe la chumvi karibu na Yahwe. [20] Itakuwa kama ishara na ushahidi
kwa Yahwe wa majeshi katika nchi ya Misri. Atawatumia mkombozi na mlinzi, na
atawokoa wao. [21] Yahwe atajulikana Misri, na Wamisri watamkubali Yahwe siku hiyo.
Watamuabudu kwa sadaka na matoleo, na wataweka agano na kulitimiza. [22] Yahwe
ataipga Misri, ataipiga na kuiponya. Halafu watamrudia Yahwe; atasikiliza maombi
yao na kuwaponya. [23] Siku hiyo kutakuwa na njia kuu kutoka Misri kwenda Asiria,
na Waasira watakuja Misri, na Wamisri watakwenda Asira; na Wamisri wataabudu
pamoja na Waasiria. [24] Siku hiyo, Israeli itakuwa ya tatu pamoja na Misri na Asiria,
baraka katikati ya nchi; [25] Yahwe wa majeshi atawabariki na kusema, " wabarikiwe
Wamisri, watu wangu; Wasiria, kazi ya mikono yangu; na Israeli urithi wangu.

# 20

[1] Katika mwaka ambao Tartani alipofika kwa Ashdodi, alipotumwa na Sarjoni
mfalme wa Asiria, nae akapigana na Ashdodd na akachukua. [2] Mda huo Yahwe
alizungumza na Isaya mwana wa Amozi, "Nenda ukaondoe nguo za magunia katika
kiuno chako, na ondoeni viatu vyenu kwenye miguu." Alifanya hivyo, tembeeni
uchi na miguu wazi. [3] Yahwe asema, "Kama ilivyokuwa kwa mtumishi wangu Isaya
alivyotembea uchi na pasipo kuvaa viatu kwa miaka mitatu, ni ishara na dalili kuhusu
Misri na kuhusu Ethiopia— [4] katika njia hii mfalme wa Asiria atawaongoza mateka
wa Misri, na walioko uhamishoni Ethiopia, watoto kwa wazee, waliouchi na wasio na
viatu, na ambao hawajajisitiri kuiweka Misri katika aibu. [5] Watafadhaika na kuona
aibu, kwa sababu ya Ethiopia ni matumaini yao na Misri ni utukufu wao. [6] Wenyeji
wa pwani hiiwatasema siku hiyo, 'Kweli, hichi ndicho chanzo chetu cha matumaini,
tulipokimbilia kuhitaji msaada kutoka kwa mfalme wa Asiria, je ni kwa jisi gani
tunaweza kupona?"

# 21

[1] Tamko kuhusu jangwa pembezoni mwa bahari. Kama dhuruba yenye upepo
inayotokea kupita Negevi kuelekea jangwani, kutoka kwenye aridhi ya kutisha.
[2] Nimepewa maono ya kusikitisha: Wasaliti wamepanga hila, na waharibifu
kuharibu. Nenda juu na uvamie, Elamu; zingira Media; Mimi nitasimamisha
maumivu yao yote. [3] Hivyo basi simba wangu wamejawa na maumivu; ni kama
mwanamke anayejifungua kwa uchungu yamenipata mimi; Nimeina chini kwa kile
nilichokisikia; nimesumbuliwa kwa kile nilichokiona. [4] Moyo wangu unajinga,
nimetitishika kwa hofu. Mapema jioni, mda wangu mzuri kwa siku, imeniletea hofu.
[5] Wameandaa meza, wametawanya vitambaa, na wanakula na kunjwa; tokea, mkuu,
pakeni ngao yenu kwa mafuta. [6] Hiili ndilo Bwana aliloniambia, "Nenda, baada ya
mlinzi; lazima atoe taarifa kwa kile atakacho kiona. [7] Kama ataona gari, jozi ya farasi,
farasi juu ya punda na farasi juu ya ngamia, hivyo basi anatakiwa kuwa makini na
kuwa macho." [8] Mlinzi analia nje, "Bwana, ninasimama juu ya mnara siku zote, kila
siku, na kwa nguzo yangu nitasimama usiku wote." [9] Tazama gari linakuja na wakiwa
wawili wawili. anaita, "Babeli umeanguka, umeanguka, na sanamu za kuchonga za

miungu yao zimevunjika chini.'' 10 Watu wangu niliwapururu na kuwapepeta, watoto
niliyewatoa kwenye sakafu yangu mwenyeweNilichokisikia kutoka kwa Yahwe wa
majeshi, Mungu wa Israeli, Nimekutangazia wewe. 11 Tamko kuhusu Duma. Mtu
mmoja amenita mimi kutoka Seiri, ''Mlinzi, ni kitu gani kilichobakizwa usiku?
12 Mlinzi akasema, ''Asubuhi itafika na vilevile usiku. Ikiwa unataka kuuliza basi
uliza; na urudi tena.'' 13 Tamko kuhusu Arabia. Katika jangwa la Arabia mmeutumia
usiku, enyi misafara ya Dedanite. 14 Leteni maji kwa wenye kiu; wenyeji wa nchi ya
Tema, waoneni watuhumiwa kwa mikate. 15 Maana wameukimbia upanga, kutoka
upanga unaotolewa, kutoka kwenye upinde ulopinda, na kutokana na uzito wa vita.
16 Maana hili ndilo Bwana alichosema na mimi, ''Ndani ya mwaka mmoja, kama mtu
aliyeajiriwa kwa mwaka ataona, utukufu wa Kedari utakwisha. 17 Ni baadhi ya ya
wavuta upinde, mashujaa wa Kader watabakia,'' maana Bwana, Mungu wa Israeli,
amesema.

# 22

1 Tamko kuhusu bonde la maono: 2 Mji wenye kelele, mji umejaa maovu; wafu
hawajauwawa kwa upanga, na hawakuuwawa kwenye vita. 3 Viongozi wenu
wamekimbia pamoja, lakini wamekamatwa pasipo na upinde, wote kwa pamoja
wamekamatwa na wamekamatwa pamoja; walikimbia kutoka mbali. 4 Hivyo
basi, Msiniangalie mimi, nitalia kwa uchungu; msijaribu kunifariji kuhusiana na
kuharibika kwa binti ya watu wangu. 5 Maana kuna siku za ghasia, akanyagaye
chini, na fujo za Bwana, Yahwe wa majeshi, katika bonge la maono, kuanguka chini
kwa ukuta, na watu wanalia juu ya milima. 6 Elamu chukua podo juu, na gari la watu
na farasi, na kirghizameweka ngao wazi. 7 Siku hiyo ambapo mabonde ulioyachagua
yatajaa magari, na farasi watachukua nafasi zao katika lango. 8 Atauodoa mbali
ulinzi wa Yuda; na utaona siku hiyo utaona silaha katika jumba la msitu. 9 Umeona
matawi ya mji wa Daudi, jinsi mlivyowengi, na kukusanya maji katika birika la
chini. 10 Umehesabu nyumba za Yerusalemu, na umerarua nyumba chini kuuimarish
ukuta. 11 Na umefanya hifadhi katika ya kuta mbili maana maji ya birika la
zamani. Maana haukuwahusisha walioujenga mji, walioupanga mji kutoka zamani.
12 Bwana, Yahwe wa majeshi amewaita siku hiyo watu waje kuomboleza na kulia,
wanyoe vichwa vyao na kuvaa nguo za magunia. 13 Lakini angalia, badala yake
sherehe na furaha, kuuwa ng'ombe na kuchinga kondoo, njooni tule na kunjwa
mvinjo maana kesho tutakufa. 14 Hili limebanika kwenye masikio yangu na Yahwe
wa majeshi: Hakika maovu haya hayatasamehewa, hata utakapokufa, ''Amesema
Bwana wa majeshi. 15 Bwana, Yahwe wa majeshi, asema hivi, ''Nenda kwa huyu
kiongozi, kwa Shebana, aliye juu ya nyumba, na umwambie, 16 Ni nina aliyekuruhusu
kuchimba kaburi lako mwenyewe, kukata juu ya kaburi na juu ya urefu katika
mahali pa kupunzikia ndani mwamba?'' 17 Yahwe anakaribia kukutupa chini;
mtu mwenye nguvu, anakaribia kukutupa chini; atakuzongazonga. 18 Atahakikisha
anatuzungusha zungusha, na kutupa msukosuko kama mpira kwenye nchi kubwa.
Pale utakapokufa, na pale gari lako tukufu litakapo kuwa; utakuwa aibu ya nyumba
ya bwana wako! 19 ''Nami nitakuondoa katika ofisi yako na katika kituo chako.
Na utavutwa chini. 20 Na itakuwa hivi kuhusu siku hiyo nitamchukua Eliakimu
mtoto wa Hilkia mtumishi wangu. 21 Nitamvisha yeye kwa kanzu yenu na kumvika
mkanda wenu, na nitahamisha mamlaka yenu kwenye mikono yake. Atakuwa baba
wa wenyeji wa Yerusalemu na katika nyumba ya Yuda. 22 Nitaziweka funguo za
nyumba ya Daudi kwenye mabega yake; Atafungua, na hakuna atakayefunga; na
atafunga na hakuna atakayefungua. 23 Nami nitamuimarisha yeye, kigingi katika
mahali salama, na atakuwa kiti cha utukufu katika nyumba ya baba yake. 24 Nao

wataangukia juu yake utukufu wote wa baba nyumba ya baba yake, watoto wake na
uzao wake na kila chombo kidogo kutoka vikombe mpaka majagi yote. 25 Siku hiyo-
hili ndilo tamko la Yahwe wa majeshi- kigingi kilichowekwa katika mazingira imara
kitatoa njia, utavunjika, na kuanguka, na uzito ulionao utaondoleawa- maana Yahwe
amesema.

# 23

1 Tamko kuhusu Tiro, Ombolezeni, enyi kondoo wa Tarishishi; 2 maana hakuna
nyumba wala bandari; kutoka katika nchi ya Kyprusi wamefunuliwa hilo. 3 Na juu ya
maji mengi ni nafaka za shiho, mazao ya Nile, na uzalishaji wao; mlikuwa wafanya
biashara wa kimataifa. 4 Kuwa na aibu, Sidoni; maana bahari imenena, mkuu wa
bahari. Amesema, ''Sijafanya kazi wala kuzaa wala kukuza vijana wadogo wala
kuwalea mabinti. 5 ''Pale taarifa ilipofika Misri, watauzunika kuhusu Tire. 6 Katiza juu
ya Tarshishi; Ole wenu, enyi wakazi wa pwani. 7 Je hili limeshawahi kuwatokea, mji
wenye furaha, ambao kwa asili yake umetoka katika kipindi cha kale. Ambapo miguu
yake imempeleka mbali kuishi kwenye maeneo ya ugenini? 8 Ni nani aliyepanga
haya dhidi ya Tire, mtoa mataji, ambao wafanyabiashara wake ni wakuu, ambao
wafanyabiashara ni watu wa kuheshimika duniani? 9 Yahwe wa majeshi amepanga
kuharibu kiburi chake na utukufu wake, na kuwahaibisha waheshimiwa wote wa
dunia. 10 Lima katika shamba lako, kama mtu alimavyo Nile, ewe binti Tarishishi.
Maana hakuna tena eneo la soko huko Tite. 11 Yahwe amenyoosha mkono wake
juu ya bahari, na ametingisha falme; na amepewa amri juu ya Fonensia, kuziharibu
ngome. 12 Amesema, ''Hamtofurahia tena, binti bikira wa Sidoni uliyenyanyasika;
nyanyuka, pitia Kyprusi; lakini wala hapatakuwa na punziko.'' 13 Tazama nchi ya
Wakaldayo. Hawa watu wamesitisha kuishi pale; Waasiria wamelifanya jangwa la
wanyama pori. Wameizingira minara; wameliharibu eneo lao; wamelifanya kuwa
chungu cha uharibifu. 14 Omboleza ewe kondoo wa Tarishishi; maana kimbilio lako
limeharibiwa. 15 Katika siku hiyo, Tire itasaulika kwa miaka sabini, kama siku za
mfalme. Baada ya miaka sabini kuisha huko Tire kutatokea kitu kama wimbo wa
malaya. 16 Chukua kinubi, nenda zunguka mji, mmewasahau malaya; cheza kinubi
vizuri, imba nyimbo nyingi, ili uweze kukumbuka. 17 Itatokea baada ya miaka
sabini, Yahwe ataisaidia Tire, na wataanza kututafuta pesa tena kwa kufanya kazi ya
umalaya, na atafanya utumishi wake katika falme za dunia. 18 Faida yake na mapato
yake yatatengwa kwa ajili ya Yahwe. Hayatahifadhiwa wala hayatakuwa na hazina,
maana faida yao watapewa wale wanoishi mdhebauni mwa Yahwe na yatatumika
kuwasambazia chakula cha kutosha na kupata mavazi yenye viwango bora.

# 24

1 Angalia Yahwe anakaribia kuifanya dunia kuwa utupu, kuhiharibu, kuharibu uso
wake, na kuwatawanya wenyeji wake. 2 Itakuwa kama ilivyo kwa watu itakuwa
hivyo hivyo kwa kuhani; na kwa watumishi na kwa bwana wake, na kwa mfanyakazi
wa ndani itakuwa hivyo na kwa tajiri yake, ndivyo itakavyokuwa kwa anayeuza na
anayenunua; ndivyo itakavyokwa kwa wenye kupata faida na wenye madeni, na wale
wennye kupokea faida itakuwa hivyo hivyo kwa wale wenye kutoa faida. 3 Dunia
itaharibiwa kabisa na kufanjwa ukiwa; maana Yahwe amenena maneno hayo. Dunia
imekauka kabisa na kunyauka, 4 Dunia inazimia n kudhohofika. Watu maarufu wa
duniani watapotezwa. 5 Dunia inavutwa na watu wakao ndani yake kwa sababu
wamepindisha sheria, wameibadili amri na wamevunja agano la milele. 6 Hivyo basi
laana inaitafuna nchi, na wenyeji wake wamekutwa na makosa. Wakaao duniani
wanateketea, na watu wachache wameachwa. 7 Divai mpya imekauka, mizabibu
imenyauka, na mioyo yote iliyochangamka inaugua. 8 Sauti ya furha ya kigoma

inasimama, na kelele za wenye furaha zimekwisha, na furaha ya kinubi imesitishwa.
[9] Hawatakunjwa mvinyo tena na kuimba, bia chungu kwa wale wanokunywa. [10] Mji
uliochafuka umeangushwa chini; kila nyumba imefungwa na hakuna kitu. [11] Kuna
kilio mtaani kwa sababu ya mvinyo; furaha yote imetiwa giza, furaha ya nchi
imetoweka. [12] Ndani ya mji kumebaki ukiwa, na lango limebolewa kwa uharibifu.
[13] Hivi ndivyo itakavyofanyika kwa dunia yote mwiongoni mwa mataifa, pale mti
wa mzabibu utakapopigwa, na waokotapo zabibu baada mavuno yake kuwa tayari.
[14] Watanyanyua saut zao na kupiga keleleYahwe mwenye enzi, na utapaza sauti
kutoka kwenye bahari. [15] Hivyo basi mashariki mtukuze Yahwe, na katika kisiwa
cha bahari tukuzeni jina la Yahwe, Mungu wa Israeli. [16] Kutoka umbali wa sehemu
ya dunia tumesika nyimbo, ''Utukufu kwa watu wenye haki! Lakini nikasema,
''Nimepita mbali, Ole juu wangu! Wasaliti walshulika na wenye hila; ndio, wasaliti
walishuhulika na wenye hila.'' [17] Hofu, shimo, na mtego yako juu yako, wenyeji wa
dunia. [18] Amekimbia maana sauti ya hofu itaanguka kwenye shimo, na anayekuja
juu katikati ya shimo atanaswa na mtego. Madirisha ya mbinguni yatafunguliwa, na
misingi ya dunia itatikisika. [19] Dunia itangamizwa kabisa, dunia itapasukia mbali;
dunia itatatikisika vikali. [20] Dunia itajikongoja kama mlevi na itachezacheza kurudi
nyuma na mbele kama kibanda. Dhambi zao zitakuwa nzito juu yao na zitaanguka na
hazitasimama tena. [21] Itakuwa siku hiyo ambayo Yahwe ataliadhibu jeshi la aliye juu
mahali pa juu, na falme za dunia katika dunia. [22] Watakusanyika pamoja, wafungwa
katika shimo, na watafungw gerezani; na baada ya siku nying watadhibiwa. [23] Halafu
Mwenzi utatiwa aibu na jua pia litatwa aibu, maana Yahwe wa majeshi atatawala
katika mlima Sayuni na Yerusalemu, kabla ya wazee wake katika utukufu.

# 25

[1] Yahwe wewe ni Mungu wangu; nitakutukuza wewe, nitalisifu jina lako; maana
umetenda matendo ya ajabu, mambo uliyoyapanga toka zamaini, kwa uaminifu
na ukamilifu. [2] Maana umeufanya mji kuwa chungu, ngome ya mji, uharibifu na
ngome ya wageni kuwa si mji. [3] Hivyo basi watu wenye nguvu watakutukuza
wewe; na mji waishio watu wasio na ukatili watakuogopa wewe. [4] Maana umekuwa
katika eneo salama kwa aliye masikni, makazi kwa mhitaji ambaye yuko kwenye
dhiki- makazi kwa aliyeko kwenye dhoruba na kivuli kwa aliyeko kwenye jua. Pale
punzi ya watu wakatili imekuwa kama dhoruba dhidi ya ukuta, [5] na jua kwenye
aridhi kavu, na watazuia kelele za wageni, kama vile jua linavyozuiliwa na kivuli
cha mawingu, hivyo basi nyimbo wasio na makosa zimejibiwa. [6] Katika mlima
huu Yahwe wa majeshi atafanya kwa watu sikukuu ya ya vitu vilivyonona, na
mvinyo uliochaguliwa, zabuni ya nyama na sikuku juu ya sira. [7] Na katika mlima
huu atauharibu mfuniko uliowekwa juu watu wote, na mtandao wa kusuka juu
ya mataifa. [8] Atameza kifo daima, na Bwana Yahwe atayafuta machozi katika
nyuso zetu; na aibu ya watu wake itatupwa mbali kutoka duniani kote, maana
Yahwe amesema hivyo. [9] Yatazungumzwa katika siku hiyo, ''Huyu ni Mungu
wetu; na tunayemngoja, na atatuokoa. Huyu ni Yahwe; tuliyemngoja, tutafurahia
na kushangilia wokovu wake.'' [10] Maana katika mlima huu mkono wa Bwana
utashuka; na Moabu itakanyagwakangwa chini kwenye eneo lake, na hata majani
yatakanyagwakanyagwa chini katika shimo lililojaa mbolea. [11] Wataitawnya mikono
yao katikati yao, kama vile mpiga mbizi atawanyavyo mikono yake wakati akipiga
mbizi. Lakini Bwana atashusha kiburi chao chini japo kuwa na ujuzi katika mikono
yao. [12] Na ataiangusha chini kwenye aridhi kuta za ngome, kwenye mavumbi.

# 26

[1] Siku hiyo wimbo huu utaimbwa katika nchi ya Yuda: Tuna mji imara; Mungu
amefanya wokovu katika kuta na ngome zake. [2] Fungua lango, ili mataifa yenye
haki yaweze na yenye kutunza imani yaweze kuingia ndani. [3] Akili mlionayo,
mtamuhifadhi yeye katika amani kamili, maana anawamini ninyi. [4] Mwamini Yahwe
daima; maana Yaha, Yahwe, ni mwamba wa milele. [5] Maana atawashusha wale
wote wenye kiburi; mji ulio juu atushusha chini, ataushusha chini kwenye aridhi;
na ataulinganisha na mavumbi. [6] Utakanyagwakanyagwa chini na miguu ya walio
masikini na wahitaji. [7] Mapito ya mwenye haki yamenyooka, Wenye haki; mapito
ya wenye haki umeyanyoosha. [8] Ndio, kaika mapito ya hukumu yako, Yahwe,
tunakusubiri wewe; jina lako na sifa zako ni matamanio yetu. [9] Nimekutamani wewe
wakati wa usiku; ndio, roho iliyo ndani yangu ina kutafuta kwa bidii. Pindi hukumu
yako itakapokuja duniani, wenyeji wa duniani watajua kuhusu haki. [10] Na tuonyeshe
upendeleo kwa waovu, lakini hawatajifunza haki. katika nchi ya wanyofu anatenda
maovu na haoni ukuu wa Yahwe. [11] Yahwe, mkono wako umenyanyuliwa juu,
lakini hawapati hizo taarifa. Lakini wataona bidii kwa watu na wataona aibu, kwa
sababu idadi ya maadui watawatafuna. [12] Yahwe, utaleta amani kwetu, maana kweli,
umekamilisha kazi zetu zote. [13] Yahwe Mungu wetu, viongozi wengine badala yako
wametutawala sisi; Lakini tunalitukuza jina lako. [14] Wamekufa, hawataishi tena;
ni maremu hao, hawatafufuka tena. Kweli, umekuja kuwahukumu na kuwaharibu
wao, na umefanya kila kumbukumbu kutoweka. [15] Umeliongeza taifa, Yahwe,
umeliongeza taifa; umeheshimiwa; umeinuliwa katika mipaka yote ya nchi. [16] Yahwe,
katika mateso yao walikuangalia wewe; walipatwa na wasiwasi katika maombi yao
maana adhabu yako ilikuwa juu yao. [17] Kama mwanamke mjamzito anayekaribia
kujifungua, hupatwa na uchungu na hulia kwa uchungu, hivyo ndivyo tulivyokuwa
kabla, Bwana. [18] Tulikuwa wajawazito, tumekuwa katika mateso, lakini ni kama
tumeshajifungua katika akili zetu. Hatujauleta wokovu duniani, na wakazi wa
duniani hawakuanguka. [19] Wafu wenu wataishi; watu wenu walio kufa watafufuka.
Amka na uimbe kwa furaha, njie muishio mavumbini; maana umande wenu ni
umande wa mwanga, na dunia itawaleta mbele wafu wake. [20] Enendeni, watu wangu,
ingieni katika vyumba vyenu na mfunge mlango nyuma yenu; jificheni kwa mda
mfupi, mpaka hasira itakapopita. [21] Maana, angalia, Yahwe anakaribia kutoka katika
eneo lake kuwahadhibu watu waishio duniani kwa ajili ya makosa yao; dunia itaachia
umwagaji wa damu, na hawatawaficha tena waliokufa.

# 27

[1] Katika siku hiyo Yahwe kwa upanga wake ulio mgumu, mkubwa na mkali,
atamadhibu Leviathani na nyoka yule anayetambaa kwa kupenya, na atamuua
mnyama anayeishi baharini. [2] Siku hiyo: Shamba la zabibu, litawaimbia. [3] ''Mimi
Yahwe ni mlinzi wake; Ninalimwagia maji kila wakati; hivyo hakuna anayelimiza,
Ninalilinda usiku na mchana. [4] Sina hasira, Oh, kama mbigiri na miiba! Katika
vita nitatembea dhidi yao; Nitawachoma wote kwa pamoja; [5] labda wafahamu
ulinzi wangu na wafanye amani na mimi, waache wafanye amani na mimi. [6] Kwa
siku inayokuja, Yakobo atachukua mzizi; Israeli itatoa maua na kuchipua; na
itaijaza aridhi yote kwa matunda.'' [7] Je Yahwe alimshambulia Yakobo na Israeli
na hayo mataifa yaliyomshambulia? Je Yakobo na Israeli waliuliwa na wao kama
mliowachinja katika mataifa mliowauwa wao? [8] Kitika kipimo halisi cha kuridhisha,
watume Yakobo na Israeli mbali; aliwaondosha mbali kwa upepo mkali, katika
siku ya upepo wa mashariki. [9] Hivyo kwa njia hii, maovu ya Yakobo yatalipiwa,
maana hii itakuwa matunda yote yakuomdolewa dhambi zake: pale atakapofanya

mathebau ya mawe kama chokaa na kuviangamiza katika vipande vipande, na
hakuna nguzo za Ashera au madhebau itakayoachwa imesimama. 10 Maana mji
imara umeharibiwa, makao yake na faragha yake yameachwa kama jangwa. Kuna
ndama wanachungwa, na huko ndiko atakapo lala na kuyala matawi yake. 11 Matawi
yake yatakaponyauka yatanguka. Wanawake watakuja na kuyatumia kutengeneza
moto, maana hawa sio watu waelewa. Hivyo basi Muumba wao hatakuwa na huruma
juu yao, na yeye aliyewaumba atakuwa na huruma juu yao. 12 Na siku hiyo itakuwa
kwamba Yahwe atapururua kutoka mto Efrate mpaka Wadi ya Misri na njie, watu wa
Israeli, tutakusanyika mahali pamoja mmoja mmoja. 13 Siku hiyo tarumbeta kubwa
litapulizwa; na watu waliopotea katika nchi ya Asiria watakuja, na waliotupwa katika
nchi ya Misri, watamuabudu Yahwe katika mlima mtakatifu huko Yerusalemu.

# 28

1 Ole kwa taji la kiburi ambalo huvaliwa na kila mlevi wa Efraimu, na ua linalofifia
la utukufu wa uzuri wake, ua lililowekwa kichwani mwa bonde linalostawi na hao
wanoshindwa na nvinyo! 2 Tazama Bwana anamtuma aliye hodari na nguvu; kama
dhoruba ya mvua ya mawe na upepo mkali unaoharibu, na atatupa kila taji la ua
chini kwenye aridhi. 3 Taji ya kiburi ya walevi wa Efraimu lililoko chini ya paa.
4 Ua lililofifia la utukufu wa uzuri wake, juu ya kichwa cha bonde la utajiri, itakuwa
kama tunda lililoiva mtini kabla ya maji yake, kwamba, wakati mtu anapoliona tunda,
wakati likiwa bado mikononi mwake, analigugumia chini. 5 Katika siku hiyo Yahwe
wa majeshi atakuwa taji nzuri na taji ya uzuri kwa watu wake waliobakia, 6 roho
ya haki kwa yeye aliyekaa katika hukumu, nguvu kwa wale waliobadilisha adui
zao katika malango yao. 7 Lakini wale wanaoyumbayumba kwa ajili ya mvinyo,
na wanojikongoja kwa ajili ya pombe kali. Kuhani na nabii watayumbayuma kwa
ajili ya pombe kali, na watamezwa na mvinjo. Watajikongoja kwa ajili ya pombe
kali, Kujikongoja katika maono na kuyumbayuma katika maamuzi. 8 Hakika, meza
zote zimejaa matapishi. Hivyo basi hakuna sehemu iliyosafi. 9 Ni nani atakaye
tufundisha maarifa, na nani atayetuelezea ujumbe? Kwa walioachishwa maziwa
au kwa wanonyonya? 10 Maana ni amri juu ya amri, utawala juu ya utawala; na
hapa kidogo na pale kidogo. 11 Kweli, kwa mdomo wa dharau na lugha za kigeni
atazungumza na watu wake. 12 Wakati uliopita aliwambia, "'Hawa ni wengine,
wape punziko walio choka; maana huku ni kujifurahisha," lakini hawakusikiliza.
13 Hivyo basi neno la Yahwe litakuwa kwao amri juu ya amri, amri juu ya amri,
utawala juu ya utawala; na kidogo hapa na kidogo pale, ili waende na kuanguka
nyuma, na kuvunjwa, kutegwa, na kukamatwa. 14 Hivyo basi sikiliza neno la
Yahwe, yeyote afaanyae maskhara, wewe unaowaongoza watu hawa ambao wako
Yerusalemu. 15 Hii itatokea kwa sababu umesema, " Tumefannya magano na kifo;
maana kuzimu wameyafikia makubaliano. Hivyo basi hukumu itakapopitishwa kwa
wingi, haitatufika sisi, maana tumefanya maneno ya uongo kuwa kimbilio letu, na
uongo kuwa makazi yetu. 16 Hivyo basi Bwana Yahwe asema hivi, "Ona: Nitaiwekea
Sayuni msingi wa mawe, jiwe la kujaribu, jiwe la pembeni lenye samani, msingi wa
uhakika. Na yeyote atayeuamini ataaibika kamwe. 17 Nitafanya haki kuwa fimbo ya
usawa, na kuwa haki pima maji. Atasafishia mbali kimbilio la waongo, na mafuriko
yatajaa balaa katika mahali pa siri. 18 Agano lako na kifo litafutwa, na makubaliano
yako na kuzimu hayatasimama. Pindi mafuriko makali yatapta, yatawazomba
njie. 19 Maana pindi yatakopita, yatawazomba nyie yatapita asubuhi na asubuhi,
na yatapita tena mchana na usiku utafika. Pale ujumbe utakapofika utasababisha
hofu. 20 Maana kitanda ni kifupi kwa mtu kunyoosha mkono wake nje, na blangeti
ni jembamba kwa yeye kujizungushia ndani" 21 Yahwe atanyanyuka kama mlima

Perazimu; Atawahimiza yeye mwenye kufanya kazi yake katika bonde la Gibeoni,
kazi ya ajabu, na kufanya matendo ya ajabu. 22 Hivyo sasa msifanye maskhara,
dhamana yako itakazwa, Nimesikia kutoka kwa Bwana, Yahwe wa majeshi, amri
ya kuiharibu nchi. 23 Kuwa tayari na sikiliza saut yangu; kuwa makini na sikiliza
maneno yangu. 24 Je mkulima anayelima siku zote kwa ajili ya kupanda, analima
tu kwenye aridhi? Je anaendelea kulima shamba lake pasipo kupanda? 25 Pindi
anapolindaa shamba lake, Je hatawanji jira ya mbegu, anapanda jira, anaweka ngano
katika mstari, shairi katika mahali pake, na yameandikw sehemu mbili? 26 Mungu
wake amemuelekeza; anamfuundisha yeye kwa busara. 27 Zaidi ya hayo, jira zile
hazipuruliwi kwa chombo kikali; wala gurudumu la kukatia linalozunguka juu ya
jira; lakini jira linapigwa kwa fimbo, na jira kwa fimbo. 28 Nafaka ni mwanzo mkate
lakini ni laini sana, japo gurudumu la gari lake na farasi wamezitawanya, na farasi
wake hawajaiponda ponda. 29 Haya yanatoka kwa Yahwe wa majeshi, yeye aliye
mshauri wa ajabu na na mwenye ubara wa hekima.

# 29

1 Ole kwa Arieli, Arieli, mji ambao Daudi ameweka kambi! mwaka hadi mwaka
unaongezeka; basi tamasha linakaribia kuja. 2 Lakini nitauzingira Arieli, na watalia
na kuomboleza; na watakuwa kwangu kama Arieli. 3 Nitaweka kambi dhidi yako
katika mzunguko, nitakuzingira kwa kuweka uzio dhidi yako. 4 Utaletwa chini
na utazungumza kutoka chini kwenye aridhi; maongezi yako yatashushwa kutoka
mavumbini. Sauti yako itakuwa kama ya pepo kwenye ardhi, na maneno yako
yatakuwa dhaifu kutoka mavumbini. 5 Jeshi la maadui wako watakuwa kama vumbi
dogo, na wingi wa wasiotisha utakuwa kama makapi yanayopita. Itatokea mara moja,
papo hapo. 6 Yahwe wa majeshi atakuja kwenu kwa radi, tetemeko la aridhi, sauti
kubwa, na upepo mkali na dhoruba kali, na mwali wa moto uteketezao. 7 Itakuwa
kama ndoto, maono ya usiku: Jeshi la mataifa yote yatapigana dhidi ya Arieli na
ngome zake. Watawavamia yeye na ngome zinazowanyanyasa wao. 8 Itakuwa
kama mtu mwenye njaa anayeota anakula, lakini pindi anapoamka tumbo halina
kitu. Itakuwa kama mtu mwenye kiu anayeota anakunywa maji, lakini anapoamka,
anazirai, kwa sababu ya kiu na sio kuizima. Ndio, itakavyokuwa idadi kubwa ya
wapiganaji dhidi ya Mlima Sayuni. 9 Shangaeni wenyewe na mjishangae; jifanye
kipofu na uwe kipofu! uwe mlevi lakini sio wa mvinyo; yumbayumba lakini sio
kwa bia. 10 Maana Yahwe ameachila roho wake katika usingizi wa kina, Ameyafunga
macho yako, manabii, na amefunika kichwa chako, waonaji. 11 Ufunuo wote umekuja
kwako kama maneno ya kitabu kilichotiwa muhuri, ambacho watu wanaweza
kumpa mtu anayejifunza, na kusema hivi, ''Soma hiki.'' na atasema, ''Siwezi
maana imetiwa muhuri.'' 12 Kama kitabu kitapewa kwa mtu asiyeweza kusoma, na
kumwambia, '''Soma hiki,'' na anasema, ''Siwezi kusoma.'' 13 Bwana asema, ''Watu
hawa wananikaribia mimi na kunishimu kwa midomo yao, lakini mioyo yao iko
mbalii na mimi. Heshima yao kwangu ni kwa sababu tu ya amri waliofundishwa.
14 Hivyo basi, tazama, Nitaendelea kufanya mambo ya ajabu mwiongoni mwa watu
hawa, maajabu baada ya maajabu. Hekima ya wenye busara itatoweka, na uelewa
wa watu wenye busara utatokomea.'' 15 Ole wao wale wanaoficha mipango yao kwa
Yahwe, na wale ambao matendo yao ni ya giza. Wanasema, ''Nani anayetuona sisi,
na ni nani anayetutambua sisi? 16 Nyie mnaebadilisha vitu juu chini! Je mfinyanzi
anaweza kufikiriwa kama udongo, hivyo basi vitu vinavyotengeneza vitasema
kuhusu aliyevitengeneza, ''Hajanitengeneza mimi, ''au vitu vinavyotngenezwa viseme
kuhusu aliyevitengeneza, Hajaelewa''? 17 Katika mda mdogo uliobakia, Lebanoni
itajeuzwa kuwa shamba, na shamba litakuwa msitu. 18 Siku hiyo viziwi watasikia

maneno ya kitabu, na macho ya vipofu yataona katika giza nene. [19] Waliodhulumiwa
watafuurahia pamoja na Yahwe, na masikini miongoni mwa watu watafurahia kwa
Mtakatifu wa Israeli. [20] Maana watu wasio katili watakwisha, na wenye dharau
watatoweka. Wale wote wanopendakuteda maovu wataondolewa, [21] nani na kwa
neno linamfanya mtu kuwa mkosaji. Watamuekea mtego kwa yeye anayeitafuta haki
katika geti na kuweka haki chini kwa uongo usio na kitu. [22] Hivyo basi Yahwe asema
hivi kuhusu nyumba ya Yakobo- Yahwe aliyemkomboa Ibrahimu, "Yakobo hataaibika
tena, wala uso wake hautabadilika rangi yake. [23] Lakini anapowaona watoto wake,
kazi ya mikono yangu, watalitakasa jina langu, Watalitakasa jina langu Mtakatifu
wa Yakobo, na wtasimama katika hofu ya Mungu wa Israeli. [24] Wale watakaopotea
kiroho watapata uelewa na walalamikaji watajifunza maarifa."

# 30

[1] Ole wa watoto waasi, "Hili ni tamko la Yahwe. "Wataweka mipango, lakini
haitatoka kwangu; wataungana na mataifa mengine, lakini hawakuongozwa na
Roho wangu, hivyo wanongeza dhambi baada ya dhambi. [2] Wanapanga kushuka
chini Misri, lakini hawajaniomba niwaelekeze. Wanatafuta ulinzi kutoka kwa Farao
kuchukua kimbilio katika kivuli cha Misri. [3] Hivyo basi ulinzi wa Farao utakuwa
aibu yenu, na kimbilio lenu katika kivuli cha Misri, kitakuwa udhalilishaji wenu,
[4] japo wakuu wako Sayuni, na wajumbe wao wamekuja Hanesi. [5] Watahaibika
kwa sababu ya watu ambao hawawezi kuwasaidia, wala kuwa na faida, lakini ni
aibu, na fedheha. [6] Tamko kuhusu mnyama wa Negevi: kupitia kwenye mlango
wa mateso na hatari, wa simba jike na simba dume, nyoka na nyoka wa moto
aneyepaa, wamebeba utajiri wao kwenye mgongo wa punda, na hazina yao katika
mabega ya ngamia, kwa watu ambao hawana msaada kwao. [7] Maana msaada Misri
hauna maana; hivyo basi nimemwita Rahabu, aliyekaa bado. [8] Sasa nenda, andika
hili mbele yao juu ya meza, na uyaandike katika kitabu, iliyaifadhiwe kwa mda
mrefu kama ushuhuda. [9] Maana ni watu waasi, watoto waongo, watoto ambao
hawaskilizi maelekezo ya Yahwe. [10] Wanawambia waonaji, "msiangalie; na kwa
manabii, "msitabiri yaliyoyakweli kwetu; zungumza maneno ya kujipendeza kwetu,
tabiri udanganyifu. Geukeni katika njia, [11] ondokeni kwenye njia; maana Mtakatifu
wa Israeli amesitisha kuongea mbele ya uso wetu. [12] Hivyo basi mtakatifu wa
Israeli asema, "Kwa sababu umekataa maneno haya na kujifunza ukandamizaji na
udanganyifu, [13] hivyo dhambi hii itakuwa kwenu kama kitu kilichovunjika tayari
kwa kuanguka, kama kitu katika ukuta mrefu ambao anguko lake linakaribia, papo
kwa hapo." [14] Atavunja kama chombo cha mfinyanyanzi kivunjavyo, hivyo basi
hakitabaki kitu, hivyo hakuna vipande vyovyote vya kigae kitoshacho kutwaa moto
jikoni, kuchota maji kisimani. [15] Maana Bwana Yahwe, Mtakatifu wa Israeli asema
hivi, "Kwa kurudi na kwa kupumzika mtaokolewa; katika utulivu na imani itakuwa
ni nguvu zako, Lakini hamkuwa tayari. [16] Amesema, 'Hapana, maana kukimbia
kwa farasi; hivyo tutakimbia; tutakimbia kwa kutumia farasi mwepesi; hivyo basi
watakaojingiza watakuwa wepesi. [17] Watu eflu moja watakimbia kwa kumuhofia
mtu mmoja; kwa vitisho vya watu watano mtakimbia mpaka mtakuwa kama nguzu
ya bendera iliyoko juu ya mlima, au kama bendera kwenye kilima." [18] Lakini Bwana
anawasubiri ili awape neema yake, Hivyo basi yuko tayari kuwaonyesha huruma.
Maana Yahwe na Mungu wa haki; Huwabarikiwe wale wanaomsubiri yeye. [19] Maana
watu wataishi Sayuni, na Yerusalemu na hawatalia tena. Hakika atakuwa neema
kwenu kwa sauti ya kilio chenu. Atakaposikia tu, atawajibu ninyi. [20] Kupitia Yahwe
tunapata mkate wa shida na maji ya mateso, hata sasa, mwalimu wako hatajifisha
mwenyewe tena, lakini utamuona mwalimu wako kwa macho yako mwenyewe.

21 Masikio yako yatasikia maneno yanayosemwa nyuma, Hii ndio njia, pitia hii,
''utakapogeuka upande wa kulia au utakageuka upande wa kushoto. 22 Mtakinajisi
kifuniko chenu mlichokiweka juu ya pesa na dhahabu na kukitupa. Mtakitupa
mbali kama hedhi kali, '''utawambia wao, ''Ondokeni hapa.'' 23 Naye atatoa mvua
kwanye mbegu zenu mtakapopanda kwenye aridhi, na mkate utakuwa kwa wingi
kutoka kwenye aridhi na mazao yatazaa kwa wingi. Katika siku hizo ng'ombe zako
zitachungwa katika eneo kubwa. 24 Ng'ombe na punda, wanaolima kwenye aridhi,
watakula chakula cha majira kilicho tawnywa kwa koleo na uma. 25 Juu ya mlima
mrefu na juu ya kilima kirefu, kutapitasha vijito na mifereji ya maji, katika siku
siku ya machinjio makuu pale minara yote itakapoanguka. 26 Mwanga wa mwenzi
utakuwa kama mwanga wa jua, na mwanga wa jua utang'aa mara saba, kama
mwanga wa siku saba. Yahwe atakapofunga kuvujwa kwa watu wake na kuyaponya
majeraha waliyoyapata. 27 jina la Yahwe limekuja kutoka sehemu ya mbali, Linawaka
kwa hasira yake na katika moshi mnene. Midomo yake imejaa hasira, na lugha yake
nia kama moto unaoangamiza. 28 Punzi yake ni kama maji yaliyojaa yanayofika
mpaka katikati ya shingo, kwa ajili kuchuja mataifa kwa kuhamasisha uharibifu.
Pumzi yake ni mzabuni katika taya za watu wanowasababisha kutangatanga mbali.
29 Utakuwa na wimbo kama usiku pale sherehe takatifu itakapofanyika, na moyo
wenye furaha, pindi mmoja atakopo kwenda na katika mlima wa Yahwe, katika
mwamba wa Israeli. 30 Yahwe atafanya mapambo ya sauti yake inayosikika na
atawaonyesha jinsi mkono wake ushukavyo na dhouba ya hasira yake na moto
uwakao, pamoja na upepo mkubwa, mvua kubwa, na mvua ya mawe. 31 Maana kwa
sauti ya Yahwe, Asiria itanyamazishwa; atahiaribu kwa fimbo. 32 Na kila adhabu
iliyochaguliwa amechagua fimbo ambayo Yahwe ataiweka juu yao na wakisidikizwa
na mziki wa kigoma na kinubi kama wataanzisha vita na kupgana nao. 33 Maana
sehemu ya kuchoma iliandaliwa toka zamani. kweli, imeandaliwa kwa mfalme, na
Mungu amelifanya kuwa na kina na upana. Rundo liko tayari kwa moto na kuni za
kutosha. Punzi ya Yahwe, ni kama mkondo kiberiti, na utawsha moto.

# 31

1 Ole wao washukao Misri kuomba msaada na kutegemea farasi, kuweka imani
katika magari (maana wako wengi) na ( maana faras haziesabiki). Lakini hawausiani
na Mtakatifu wa Israeli, wala hawamtafuti Yahwe! 2 Lakini ni mwenye busara, na
ataleta maafa na atakanusha maneno yake. Na atakuja juu ya nyumba zitendazo
maovu, na dhidi ya wale wanaowasaidia kuteda dhambi. 3 Misri ni mtu na sio Mungu,
ni farasi wa mwili na sio wa roho. Yahwe atakapota nje kwa mkono wake, wote
waliowasaidia watakuwa na mashaka, na yeyote atakayesidia atanguka; wote kwa
pamoja watatoweka. 4 Hivi ndivyo Yahwe alivyosema na mimi, '' kama simba, na
hata mtoto wa simba, hunguruma juu ya mawindo yake, pale makundi ya wachungaji
yanapoita dhidi yake, lakini hatatemeka kwa sauti zao, wala hatakwenda kwa sababu
ya kelele zao, hivyo Yahwe wa majeshi atashuka kupigana kwenye mlima Sayuni,
katika kilima hicho. 5 Kama ndege apaavyo, hivyo Yahwe wa majeshi atailinda
Yerusalemu; atailinda na kuiokoa kama apitavyo juu na kuilinda. 6 Mrudieni yeye
kutoka huyo mliyemgeukia, watu wa Israeli. 7 Maana katika siku hiyo kila mmoja
ataondoa miungu ya fedha na miungu ya dhahabu iliyotegenezwa kwa mikono yenu
yenye dhambi. 8 Asiria atangamizwa kwa upanga; na upanga usioshikiwa na mtu
utumaliza yeye. Ataukimbia upanga, na vijana wake wadogo watafanyishwa kazi
ngumu. 9 Na watashindwa kujiani kwa sababu ya hofu, na mkuu wao ataogopa mbele
ya bendera ya jeshi la Yahwe.''- Hili ni tamko la Yahwe, ambao moto uko Sayuni na
ambayo sufuria ya moto iko Yerusalemu.

# 32

1 Tazama, mfalme atatawala kwa haki, wakuu wataongoza kwa haki. 2 Kila mmoja
atakuwa kama makazi kutoka kwenye upepo na kimbilio kutoka kwenye dhoruba,
kama mifereji kwenye sehemu kavu, kama kivuli kwenye mwamba mkubwa katika
nchi iliyochoka. 3 Halafu macho ya waie wanaoona hayataona giza, na masikio ya
wale wanosikia yatasikia vizuri. 4 Wenye upele watafikiria kwa makini kwa uelewa
wao, na wenye kigugumizi watazungumza dhahiri na kwa urahisi. 5 Mjinga hataitwa
tena muheshimiwa, wala muongo hataitwa mkuu. 6 Maana mjinga anazungumza
ujinga, na moyo wake unapanga maovu na matendo ya wasiomcha Mungu, na
anaongea mambo mabaya kuhusu Yahwe. Na anawafanya wenye njaa kuwa tupu na
wenye kiu kukosa maji 7 Njia ya muongo ni maovu. Anajua kubuni mipango mibaya
ya kuwalagai masikini kwa uongo, na hata kama masikini atazungumza ukweli.
8 Lakini watu wa heshima wanapanga mipango ya kuheshimika; na kwa sabaubau
ya matendo ya wenye heshima tuatasimama. 9 Nyanyukeni juu, enyi wanawake
mlio wepesi, na sikilizeni sauti yangu; enyi mabinti msiowangalifu, nisikilizeni
mimi. 10 Maana kwa mda mfupi zaidi ya mwaka ujasiri wenu utavunjika, nyie
wanawake msiojali, maana mavuno ya zabibu yatakwama, mavuno hayatakuwepo.
11 Tetemekeni, enyi wanawake, mliowadhaifu; taabikeni enyi msikuwa wangalifu;
ondoeni nguo zenu nzuri mbaki wazi; 12 Vaeni nguo za magunia katika viuno vyenu.
Ole watakaojichukulia mashamba mazuri, kwa mzabibu ulio zaa sana. 13 Kwenye
aridhi ya watu wangu kutamea miiba na mbigiri, hata juu ya nyumba za furaha
na mji ulio na shangwe. 14 Maana jumba litaachwa, mji uliosongamana utakuwa
faragha; kilima na mnara vitakuwa mapango daima, furaha ya punda, malisho
ya mifugo; 15 mpaka roho itushukie sisi kutoka juu, na jangwa litakuwa shamba
linalozaa, na shamba linalozaa litachukuliwa kama msitu. 16 Wenye haki wataishi
jangwani; na wenye haki wataishi katika shamba linalozaa matunda. 17 Kazi ya
mwenye haki itakuwa ni ya amani; na matokeo ya wenye haki, ni utulivu na
kujiamini daima. 18 Watu wangu wataishi katika makao ya amani, na katika nyumba
salama na mahali tulivu pa kupumzikia. 19 Lakini hata kama ni mvua ya mawe na
msitu umeharibiwa, na mji umeteketezwa, 20 yule ambae anaye panda pembezoni
mwa mifereji atabarikiwa, na yule atakaye wapeleka ng'ombe na punda kuchunga.

# 33

1 Ole wenu, waharibifu ambao hamjaharibiwa! Ole wao wasaliti ambao ham-
jaslitiwa! Pindi mtakapoacha uaribifu, nanyi mtaharibiwa. Pindi mtakapoacha
usaliti, nayi mtasalitiwa. 2 Yahwe, tuurumie sisi; tumekusubiri wewe; umekuwa
mkono wetu kila asubuhi, na wokovu wetu katika kipindi cha mateso. 3 Watu
wamekimbia kwa kusikia sauti kubwa; uliponyanyuka, mataifa yametawanyika,
4 Mateka wako wamejikusanya kama mkasanyiko wa nzige; kama nzige warukavyo,
watu wataruka juu yake. 5 Yahwe ameinuliwa. Anaishi mahali pa juu. Ataijaza
Sayuni kwa haki na usawa. 6 Atakuwa imara katika kipidi chenu, wingi wa wokovu,
busara, na maarifa; hofu ya Yahwe iko katika hazina yake. 7 Tazama, wujumbe
wanalia mtaani; wanadiplomasia wanamatumaini ya amani kwa kulia kwa uchungu.
8 Barabara kuu imeachwa faragha; hakuna wasafiri tena. Maagano yamevujika,
mashahidi wanadharaulika, na utu wa mtu hauheshimiki. 9 Nchi imeomboleza na
kunyaukia mbali; Lebanoni inaibisha na kunyaukia mbali; Sharoni imekuwa kama
jangwa wazi; Bashani na Kermeli zimepuputisha majani yake. 10 ''Sasa nitanyanyuka,
''asema Yahwe; '' sasa nitanyanyuliwa juu; sasa nitainuliwa. 11 Utashika mimba
ya makapi na utazaa mabua; na punzi yako ni moto ambao utakuunguza wewe.
12 Watu watachomwa na kuwa kama chokaa, kama miiba ya porini inavyokatwa

na kuchomwa. 13 Enyi mlio mbali sana, sikiliza nilicho kifanya; na enyi mlio
karibu, kirini ukuu wangu.'' 14 Watenda zambi wa Sayuni wanogopa; tetemeko
limewakuta wasio na Mungu. Ni nani miongoni mwetu anayeweza kukaa kwenye
moto mkali? Na ni nani miongoni mwetu anayeweza kukaa kwenye moto wa
milele? 15 Nyie mnaotembe katika haki na kuongea kw uaminifu; yeye anayedharau
mapato ya ukandamizaji, yeye anayekataa kuchuka rushwa, ambaye hausiki kwenye
kupanga vurugu za kihalifu, na ambaye haangali maovu- 16 Ataiweka nyumba yake
juu; sehemu yake ya ulinzi itakuwa ni ngome ya mwamba; chakula na maji yake
hayataisha. 17 Macho yako yatamuona mfalme katika uzuri wake; watatazama
nchi kubwa. 18 Moyo wako utakumbuka hofu; yuko wapi mwandishi, yuko wapi
yule aliayepima pesa? na yuko wapi yeye aesabue minara? 19 Hautawaona watu
wanaopinga, watu weye lugha ya ajabu ambayo hautaweza kuielewa. 20 Itazame
Sayuni, mji wa sikukuu yetu; macho yako yataiona Yerusalemu kama makao tulivu,
hema ambalo halitatolewa, vigingi vyake havitatolewa wala kamba zake hazitakatika.
21 Badala yake Yahwe katika ukuu wake atakuwa pamoja na sisi, katika eneo la
maji mengi na mifereji mingi. Hakuna manuari na mpiga makasia watakayepita
hapo, na hakuna mashua itakayopita uko. 22 Maana Yahwe ni hakimu wetu, Yahwe
ni mwanasheria wet, Yahwe ni mfalme wetu; atatukomboa sisi. 23 Kamba zako
zimelegea; haziwezi kushika mlingoti katika eneo lake; haziwezi kuzunguka meli;
pindi mateka wanavyogawanyika, hata vilema watawatoa nje kama mateka. 24 Na
wenyeji watasema, ''Ninaumwa;'' watu wanaoishi pale watasamehewa maovu yao.

# 34

1 Njooni karibu enyi mataifa, sikilizeni na muwe makini, enyi watu! Dunia na
vyote vijazavyo vinatakiwa kusikiliza, dunia na vyote vitokavyo, 2 Maana Yahwe ana
hasira na mataifa yote, ana hasira dhidi ya majeshi yao; amewaangamiza wao kabisa,
ameawakabidhi kwa wachinjaji. 3 Miili ya watu wao waliokufa itatupwa nje. Harufu
ya miili iliyokffa itakuwa kila mahali; na mlilima italowekwa kwa damu yao. 4 Nyota
zote angani zitafifia, na anga litakunjwa kama kitabu; na nyota zake zitafifia mbali,
kama tawi linavyonyauka kwenye mzabibu, kama tunda lilokomaa kwenye mti.
5 Maana pale upanga wangu utakapokunywa na kushiba mbinguni; tazama, maana
sasa utakuja chini huko Edomu, kwa watu ambao nimewaweka mbali na adhabu.
6 Upanga wa Yahwe unadondosha matone ya damu na kufunikwa kwa mafuta,
matone ya damu ya kondoo na mbuzi, yamefunikwa kwa figo za kondoo. Maana
Yahwe ametoa sadaka katika Bozra na mauwaji katika nchi ya Edomu. 7 Ng'ombe
wa porini watachinjwa pamoja na wao, fahali wakubwa na fahali wadogo. Nchi yao
italewa kwa damu, na mavumbi yake yatafanjwa kuwa mafuta na mafuta yaliyonona.
8 Maana itakuwa ni siku ya kisasi kwa Yahwe na mwaka ambao anawalipa kwa
sababu ya Sayuni. 9 Mifereji ya Edomu itageuka kuwa lami, na mavumbi yake
yatakuwa kiberiti na nchi itakuwa kama lami inayoungua. 10 Itaungua usiku na
mchana; moshi wake utatoka daima; na patakuwa nyika kizazi hata kizazi; na hakuna
hata mmoja atakayepita hapo milele na milele. 11 Lakini ndege na wanyama porini
wataishi pale; bundi na kunguru watatengeneza viota vyao pale. Atanjoosha juu
yake futi kamba ya uharibifu na pima maji ya uharibifu. 12 Wenye vyeo hawatakuwa
na kitu kilichobakia kuita ufalme, na wakuu wote watakuwa si kitu. 13 Miiba itaota
katika maeneo yao, viwavi na mbigiri vitakuwa katika ngome zao. Yatakuwa makao
ya mbweha, makazi ya mbuni. 14 Wanyama wa porini na fisi watakusanyika pale,
na mbuzi wa porini watalia wao kwa wao. Nyakati za usiku wanyama watakaa
pale na watajitafutia wenywe mahali pa kupumzikia. 15 Bundi watatengeneza viota
vyao, na kutotolea mayai yao, kila mmoja na mwenzake. 16 Kutafuta kupitia kitabu

cha Yahwe; hakuna hata kimoja ambacho hakitakuwepo. Hakuna kitakacho kosa
mwenzake; maana mdoma wake umeamuru hivyo, roho yake imewakusanya wao.
17 Atapiga kura katika eneo lao, na mkono wake umewapima kwa kamba. Wataimiliki
daima; kutoka kizazi hata kizazi wataishi pale.

# 35

1 Jangwa na Arabu watafurahia; na jangwa litafurahia na kuchanua. Kama waridi,
2 Yatachanua kwa wingi na yatashangilia kwa furaha na nyimbo; litapewa utukufu
wa Lebanoni, mapambo ya Karmeli na Sharoni; watauona utukufu wa Yahwe,
mapambo ya Mungu wetu. 3 Itieni nguvu mikono iliyo dhaifu, na badala ya magoti
yanayotingishika. 4 Waambie wenye moyo wa uwoga, "Wawe imara, wasiogope!
Tazama, Mungu wako anakuja na kisasi, kwa ajili ya malipo ya Mungu. Atakuja
na kutuokoa." 5 Halafu macho ya vipofu yataona, na masikio ya viziwi yatasikia.
6 Halafu kilema atarukaruka kama kulungu, na ulimi wa bubu utaimba, maana maji
yatabubujika Araba, na mifereji jangwani. 7 Mchanga ulioungua utakuwa kisima,
na aridhi iliyo na kiu itakua chemchem; katika makazi mbweha, pale waliopokuwa
wanaishi, kutakuwa na nyasi pamoja na mianzi. 8 Barabara kuu itaitwa Njia takatifu.
Wasio safi hawatasifiri kwa kutumia njia hiyo. Lakini itakuwa kwa ajili ya mtu
yeyote anayetembea juu yake. Hakuna mjinga atakayeipitia. 9 Hakuna simba
pale, wala mnyama mkali katika barabara hiyo; hawatakuwepo kabisa pale, lakini
waliokombolewa watapita pale. 10 Fidia ya Yahwe itarudi na itakuja kwa wimbo
wa Sayuni, na furaha ya milele itakuwa katika vichwa vyao; furaha na shangwe
vitawazidi wao; huzuni na magonjwa yataondoshwa mbali.

# 36

1 Katika mwaka wa kumi na nne wa mfalme Hezekia, Senacherebi, mfalme wa
Asiria, alivamia miji yote ya Yuda na kuwakamata. 2 Halafu mfalme wa Asiria
akamtuma kamanda mkuu na jeshi kubwa kutoka Lachishi mpaka Yerusalemu kwa
mfalme Hezekia. Alipofika kwenye mfereji katika kisima cha juu, katika njia kuu
na katika shamba la dobi na akasimama pale. 3 Maofisa wa Israeli waliotumwa
kuzungumza nao walikuwa ni Eliakimu mtoto wa Hilkia, kiongozi wa jumba, Shebna
katibu wa mfalme, na Joa mtoto wa Asapha, anayeandika makubaliano ya serekali.
4 Kamanda mkuu wa jeshi akawaambia wao, "Mwambieni Hezekia kwamba mfalme
mkuu, mfalme Asiria, asema, 'Nini chanzo cha ujasiri wako? 5 Unaongea maneno
yasiyo na maana tu, nasema kama kuna shauri na nguvu za vita. Sasa ni nani
unayemuamini? na ni nani aliyekupa ujasiri wa kuniasi mimi. 6 Tazama, umeweka
imani yako Misri, maana banzi la mwanzi unalolitumia kama fimbo ya kutembelea,
ikiwa mtu ataiegemea na kuishika kwenye mkono wake itamchoma. Hivyo ndovyo
jinsi Farao mfalme wa Misri alivyo kwa yeyote anayemuamini. 7 Lakini ikiwa
utasema nami, "Tunamwamini Yahwe Mungu wetu,"Je sio yeye ambaye Hezekia
ameondosha mahali palipoinuka na madhebau, asema kwa Yuda na Yerusalemu,
"Lazima tuabudu mbele ya madhebau hii katika Yerusalemu"? 8 Hivyo sasa, nataka
kukufanya wewe kuwa zawadi nzuri kwa Bwana mfalme Asiria. Nitakupa farasi elfu
mbili, kama utaweza kuwatafutia dereva. 9 Ni kwa jinsi gani unaweza kumpinga
moja kati ya nahodha aliye mdogo katika watumishi wa Bwana wangu? Mmeweka
imani yenu Misri katika gari na farasi! 10 Halafu sasa, Je nimewezaje kusafiri mpaka
hapa pasipo Yahwe kupigana dhidi ya nchi hii na kuhiaribu? Yahwe asema nami,
Vamia nchi hii na uhiharibu. 11 Halafu Eliakimu mtoto wa Hilkia, na Shebna na
Joa asema kwa kamanda mkuu, Tafadhali zungumza na watu wako kwa lugha ya
kiashuru, maana kiashuru tunakielewa. Usiongee na sisi kwa lugha kiyahudi katika

masikio ya watu ambao wako ukutani." [12] Lakini kamanda mkuu akasema, "Je bwana
wenu ametuma kwa bwana wako na kuzungumza haya maneno? Je hajanituma kwa
watu walio kaa kwenye ukuta, ili wale kinyesi chaao mwenyewe na kunywa mkojo
waomwenyewe? [13] Halafu kamanda mkuu akasimama na kupiga kelele kwa sauti
kubwa kwa lugha ya kiyahudi, na akisema, [14] "Mfalme asema, ' Msimruhusu Hezekia
awadanganye ninyi, maana hataweza kuwaokoa ninyi. [15] Msimruhusu Hezekia
awafanye muumuamini Yahwe, Nawambieni Hakika Yahwe atatukomboa sisi; mjii
huu hautachukuliwa na mfalme wa Asiria." [16] Msimsikilize Hezekia, maana hivi
ndivyo mfalme wa Asiria anavyosema: 'Fanyeni amani na mimi na mje kwangu.
Halafu kila mmoja wenu atakula kwenye mzabibu wake mwenyewe na tunda la
mti wake mwenyewe, na kunjwa maji ya kisima chake mwenyewe. [17] Mtafanya
hivi mpaka nije kuwachukua na kuwapeleka kwenye nchi kama ya kwenu. nchi
ya mavuno na mvinyo mpya, nchi ya mkate na shamba. [18] Msimruhusu Hezekia
awapotoshe nyie, akisema, Yahwe atatuokoa nyie; Je kuna miungu ya aina yeyote ya
watu iliyowakomboa kutoka mikononi mwa mfalme wa Asiria? [19] Wako wapi miungu
wa Hamathi na Arpadi? Iko wapi miungu ya Sefarvaimu? Je wameikomboa Samaria
kutoka kwenye nguvu zangu? [20] Miongoni mwa miungu yote ya nchi hii, Je kuna
miungu ya aina yeyote iliyoikomboa nchi yao kutoka kwenye nguvu yangu, ni kama
Yahwe anaweza kuawokoa Yerusalemu kutoka kwenye nguvu yangu?" [21] Lakini watu
wanabaki kimya na hawataki kujibu, maana amri ya mfalme ilikuwa, "Msimjibu".
[22] Halafu Eliakimu mtoto wa Hilkia, yeye aliye juu ya kaya, Shebna mwandishi,
na Joa mtoto wa Asafu, na mtunza kumbukumbu, walikuja kwa Hezekia na nguo
zilizotoboka na wakapeleka maneno ya kamanda mkuu.

# 37

[1] Ikawa siku hiyo mfalme Hezekia aliposika taarifa zao, alichana mavazi yake,
na kujifunika nguo za magunia, na akaenda kwenye nyumba ya Yahwe. [2] Na
alimtuma Eliakimu, ambae ni kiongozi wa kaya na Shebna mwandishi, na wazee
wa makuhani, wote walijifunika nguo za magunia, kwa Isaya mtoto wa Amozi, nabii.
[3] Wakamwambia yeye, Hezekia akasema hivi, 'Siku hii ni siku ya dhiki, kukemewa,
na aibu, ni kama mtoto aliye tayari kuzaliwa lakini mama yake hana nguvu za
kumsukuma mtoto. [4] Itakuwa Yahwe Mungu wenu atasikia maneno ya kamanda
mkuu, ambao mfalme wa Asira Bwana wake alimtuma kumpinga Mungu anayeishi,
na atakemea maneno ambayo Yahwe Mungu wenu ameyasikia. Sasa inueni maombi
yenu juu mabaki yaliyoobakia hapa." [5] Sasa watumishi wa mfalme Hezekia walikuja
kwa Isaya, [6] na Isaya akawambia, "Mwambieni Bwana wenu: 'Yahwe amesma,
"Msiogope kwa maneno mliyoyasikia, maneno ambayo mfalme wa Asiria amenitusi
mimi. [7] Tazama nitaiweka roho yangu ndani yake na atasikiliiza taarifa fulani na
atarudi kwenye nchi yake mwenyewe. Na nitamfanya anguke kwa upanga katika
nchi yake mwenyewe." [8] Basi kamanda mkuu alirudi na kumkuta mfalme wa Asira
anapigana dhidi ya Libna, Maana aliskia kwamba mfalme amekwenda mbali kutoka
Lachishi. [9] Halafu Sennacheribi alisikia kwamba Tirkhaka mfalme wa Ethiopia
na Misri wamehamasishana kupigna dhidi yake. Hivyo akamtuma mjumbe mara
nyingine kwa Hezekia apeleke ujumbe: [10] "Mwambie Hezekia, mfalme wa Yuda,
'Usimruhusu Mungu unayemwamini akudanganye, "Yerusalemu haitatiwa mikononi
mwa mfalme wa Asiria." [11] umesikia kitu ambacho mfalme wa Asiria alichokifanya
kwa nchi yote kwa kuiangamiza kabisa. Je utawaokoa? [12] Je miungu ya mataifa
imewakomboa? taifa ambalo baba yangu aliliangamiza: Gozani, Harani, Rezefi na
watu wa Edeni katika Telassari? [13] Yuko wapi mfalme wa Hamathi, mfalme wa
Arpadi, mfalme wa miji ya Sefarvaaimi, wa Hema na Ivva?" [14] Hezekia alipokea

barua hii kutoka mikononi mwa mjumbe na kisoma. Halafu akaenda juu kwenye
nyumba ya Yahwe na kuusoma mbele yake. [15] Hezekia alimuomba Mungu: [16] Yahwe
wa majeshi, Mungu wa Israeli, wewe ambae uko juu ya makerubi, wewe ni Mungu
mwenywe juu falme zote za dunia. umezifanya mbingu na nchi. [17] Jeuza masikio
yako, Yahwe, na sikiliza. Fungua macho yako, Ee Yahwe na uone, na usikilize
maneno ya Sanacheribi, ambayo ameyatuma kumfanyia mzadha Mungu anayeishi.
[18] Ni kweli Yahwe, mfalme wa Asiria ameangamiza mataifa yote na aridhi yao.
[19] Wameiweka miungu yao katika moto, maana haikuwa miungu lakini kazi ya
mikono ya wanadamu, ni kuni na jiwe tu. [20] Hivyo Waasira wameawaangamiza wao.
hivyo saa Yahwe Mungu wetu, tuokoe kwa nguvu zako, ili falme zote za duniani
zijue kwamba wewe ni Yahwe peke yako." [21] Basi Isaya mtoto wa Amozi alituma
ujumbe kwa Hezekia, na kusema, Yahwe Mungu wa Israeli amesema, Kwa sababu
umeomba kwangu kuhusu Sannacheribi mfalme wa Asiria, [22] Haya ndiyo maneno
ambayo Yahwe amezungumza kuhusu yeye, "Binti bikira wa Sayuni wanakudharau
na kukucheka kwa dharau; mabinti wa Yerusalemu wanatingisha vichwa vyao kwa
ajili yako. [23] Ni nani unayempinga na kumtusi? na dhidi ya nani unayenyanyua
sauti yako na kunyanyua macho yako kwa kiburi? dhidi ya mtakatifu wa Israeli.
[24] Kwa kupitia watumishi wako umempinga Bwana na amesema, 'Kwa wingi wa
gari nimepanda juu kwenye kilele cha milima, katika kilele cha mwuinuko wa
Lebanoni. Nitaikata mierezi yake na kuchagua miti ya miseprasi pale, ni msitu uzao
sana. [25] Nimechimba kisima na kunywa maji; nimechimba mito yote ya Misri chini
ya nyayo za miguu yangu.' [26] Je haujasikia jinsi nilivyoamua toka siku nyingi na
nimelifanyia kazi toka kipindi cha kale? ninayaleta sasa ili yaweze kutimia. Mko
hapa kuhiaribu miji imara na yenye ulinzi wa kutosha na kuwa chungu cha uharibifu.
[27] Wakazi wake, waliowadhaifu, waliokata tamaa na wenye aibu. Wanaotesha
shambani, majani mabichi, majani juu paa au kwenye shamba kabla ya upepo wa
mashariki. [28] Lakini najua kukaa kwenu chini, kutoka kwenu nje, mnapoingia ndani,
na mnapokuwa wakali dhidi yangu. [29] Kwa sababu mnakuwa wakali dhidi yangu,
maana kiburi chenu kimeyafikia masikio yangu, Nitaweka ndoano katika pua zenu,
na sauti katika midomo yenu; Nitawageuza nyuma kwenye njia mliyokuja nayo.
[30] Hii itakuwa wimbo kwenu: mwaka huu mtakula kinachoota porini na mwaka
pili mtakula kinachoota hapo hapo. Lakini mwaka wa tatu lazima mpande na
mvune, pandeni mizabibu na mle matunda yake. [31] Mabaki ya nyumba ya Yuda
ambao wanaishi watachukua mzizi tena na kuzalisha matunda. [32] Maana katika
Yerusalemu waliobaki watatoka; Kutoka kwenye mlima Sayuni waliobaki watakuja.
Bidii ya Yahwe wa majeshi itafanikisha hili." [33] Hivyo basi Yahwe asema hivi kuhusu
Asiria: "Atakuja katika miji, wala kurusha mkuki hapa. Wala atakuja hapa mbele
kwa ngao au kujenga uzio njia panda dhidi yao. [34] Njia atakayojia itakuwa njia
hiyo hiyo atakayorudia; ataingia katika mji huu. Hili ni Tamko ya Yahwe. [35] Maana
nitaulinda huu mji na kuuokoa, kwa niaba yangu mimi mwenyewe na kwa niaba
Daudi mtumishi wangu." [36] Halafu malaika wa Yahwe alienda nje na kuvamia kambi
ya Waasiria, na kuwauwa askari 185, 000. Watu walipoamka asubuhi na mapema,
miili iliyokufa imelala kila mahali. [37] Hivyo Sennacheribi mfalme wa Asiria aliiacha
Israeli na kwenda nyumbani na akakaa Ninewi. [38] Baadaye, na alipokuwa anabudu
katika nyumba ya Nisrochi mungu wake, mtoto wake Adramaleki na Shareza alimuua
kwa upanga. Halafu wakakimbilia kwenye nchi ya Ararati. Halafu Esarhadoni mtoto
wake akatawala katika sehemu ya baba yake.

## 38

[1] Siku zile Hezekia alikuwa anaumwa karibia na kufa. Hivyo Isaya mtoto wa Amozi,

nabii alikuja kwake na kumwambia, ''Yahwe amesema, 'panga mambo yako maana
utakufa, hautaishi.' [2] 'Halafu Hezekia akaugeukia ukuta na akamuomba Yahwe. [3] Na
akasema, ''samahani Yahwe, kumbuka jinsi nilivyoenenda kwa uaminifu mbele zako
kwa moyo wangu wote, na jinsi nilivyofanya matendo mema katika macho yako.'' Na
Hezekia akalia kwa sauti. [4] Basi neno la Yawe likamjia Isaya, na kusema, [5] ''Nenda
ukamwambie Hezekia, kiongozi wa watu wangu, ''Hivi ndivyo Yahwe, Mungu wa
Daudi babu yenu, amesema: Nimeyasikiliza maombi yako, na nimeyaona machozi
yako. Ona ninakaribia kuongeza miaka kumi na tano katika maisha yako. [6] Na
nitakukomboa wewe pamoja mji huu kutoka kwenye mkono wamfalme wa Asiria, na
nitaulinda huu mji. [7] Na hii itakuwa alama kwako kutoka kwangu, Yahwe, kwamba
nitafanya nilichokisema: [8] Angalia, nitasababisha kimvuli katika nyumba ya Ahazi
kwenda nyuma hautua kumi.'' hivvyo basi kivuli kilirudi nyuma hatua kumi juu ya
nyumba iliyopanda juu. [9] Haya ndiyo maandishi ya maombi ya Hezekia mfalme
wa Yuda, alipokuwa anaumwa halafu akapona: [10] ''Nimesema kwamba nusu ya
maisha yangu nitapita katika mlango wa kuzimu; Nilitumwa pale miaka yangu yote.
[11] Nikasema sitamuona tena Yahwe, Yahwe kaika nchi ninayoishi; sitaangalia watu
tena au wenyeji wa dunia hii. [12] Maisha yangu yameondolea na kupelekwa mbali
na mimi kama hema la mchungaji; Niliyakunja maisha yangu juu kama mfumaji;
ameniondoa katika kifungo; kati ya mchana na usiku ameyakomesha maisha yangu.
[13] Nililia mpaka asubuhi; kama simba anaivunja mifupa yangu. Kati ya usiku na
mchana ameyakomesha maisha yangu. [14] Kama mbayuwayu ndivyo nilivyolia; nililia
kama njiwa; macho yangu yalichoka kuangalia juu. Bwana ninateseka; nisaidie mimi.
[15] Niseme nini? wote wameongea na mimi na amefanya hivyo; Nitatembea taratibu
miaka yangu yote maana ninayashinda kwa huzuni. [16] Bwana, mateso uliyoyatuma ni
mazuri kwangu; ikiwezekana nirudishiwe tena maisha yangu; umeyahifadhi maisha
maisha yangu na afya yangu. [17] Ni kwa faida yangu kwamba nimwpitia huzuni
kama hii. Umenikomboa kutoka kwenye shimo la uharibifu; maana umetupa dhambi
zangu nyuma yako. [18] Maana kuzimu hapata kushukuru wewe; kifo hakikusifu
wewe; wale wote waendao ndani ya shimo hawana matumaini ya uaminifu wako.
[19] Mtu anayeishi, mtu anayeishi, ndiye anayekushukuru wewe, kama ninavyofanya
leo; baba atawjulisha watoto uaminifu wako. [20] Yahwe anakarbia kunikomboa mimi,
na tutasherekea kwa mziki siku zote za maisha yetu katika nyumba ya Yahwe.''
[21] Sasa Isaya alisema, ''Waacheni wachukue donge mitini na kuliweka kweye jipu
naye atapona. [22] ''Hezekia pia alisema, ''Je ni ishara gan ya kwamba nitaiende juu
katika nyumba ya Yahwe?''

# 39

[1] Katika mda ule Merodaki mtoto wa Baladani, mfalme wa Babeli, alituma zawadi
na barua kwa Hezekia; maana alisikia Hezekia alikuwa anaumwa na amepona.
[2] Hezekia alifurahishwa na hivi vitu; alimuonyesha mjumbe nyumba ya ghala la vitu
vya thamani- vitu kama fedha, dhahabu, viungo, na mafuta ya thamani, ghala la
kuwekea silaha zake, na vitu vyote vilivyopatikana kwenye stoo yake. Hapakuwa
na kitu katika nyumba yake, wala ufalme wake wote, Hezekia hakuwaonyesha
wao. [3] Basi Isaya nabii alikuja kwa mfalme Hezekia na kumuuliza, ''Je watu hawa
wamekuambia nini? wametoka wapi?, ''Wamekuja kwangu kutoka mbali nchi ya
Babeli.'' [4] Isaya akamuuliza je ni vitu gani walivyoviona katika nyumba yako?
Hezekia akajibu, ''Wameona kila kitu katika nyumba nyangu. Hakuna kitu miongoni
mwa vitu vyangu vya thamani ambavyo sijawaonyesha.'' [5] Basi Isaya akamwambia
Hezekia, ''Sikiliza neno la Yahwe wa majeshi: [6] 'Tazama siku inakaribia kuja pale
kila kitu katika nyumba yako, vitu ambavyo mababu zako wamevihifadhi mbali

mpaka mda huu wa sasa Vitapelekwa Babeli. Hakuna kitakachobakizwa, asema
Yahwe. 7 Na watoto watazaliwa kutoka kwako, ambao wewe mwenyewe utawazaa-
watachukuliwa mbali, na watakuwa matoashi katika jumba la mfalme wa Babeli."
8 Basi Hezekia akamwambia Isaya, "Neno la Yahwe alilolizunumza ni zuri." Maana
alifikiria, "Patakuwa na amani na utulivu katika siku zangu."

# 40

1 "Faraja, faraja watu wangu," amesema Mungu. 2 "Ongea kwa upole kwa
Yerusalemu; na tangaza vita vimeisha, maana maovu yao yamesamehewa, maana
alipokea mara mbili kutoka kwa mkono wa Yahwe kwa dhambi zao." 3 Sauti inalia
nje, "Katika jangwa tengeneza njia ya Yahwe; njoosha njia ya Araba katika njia kuu
ya Mungu." 4 Kila bonde litanyanyuliwa juu, kila mlima na kilima kitasawazishwa;
na aridhi ya mwinuko itasawazishwa, mahali palipokwaruzwa patakuwa na usawa;
5 na utukufu wa Mungu utafunuliwa, na watu wote wataona kwa pamoja; maana
mdomo wa Yahwe umezungumza. 6 Sauti inasema, "Lia." Jibu lingine, "Kwa nini
nilie?" "Mwili wote ni nyasi na maagano yaliyoaminika ni kama ua kwenye shamba.
7 Nyasi zinanyauka na maua yanaperuka pale Yehwe atakapo puliza punzi yake
juu yake; hakika ubinadamu ni nyasi. 8 Nyasi hunyauka, maua hupepea, lakini
neno la Yahwe litasimama daima." 9 Nenda juu ya mlima mrefu, Sayuni, mbeba
taarifa njema. waambie miji ya Yuda, "Hapa ni Mungu wako!" 10 Angalia, Bwana
Yahwe anakuja kama mpiganaji shujaa na jeshi imara linatawa juu yake. Ona,
zawadi yako iko kwake, na wale walikombolewa wataenda mbele yake. 11 Atalilisha
kundi lake kama mchungaji, Atawakusanya kondoo katika jeshi lake, na kulichukua
karibu na moyo wake, kwa upole atawongoza wake kuwauuguza watoto wao. 12 Ni
nani aliyepima maji ya mashimo kwa mkono wake, anayepima anga kwa urefu wa
mkono wake, na kuweka vumbi za nchi katika kikapu, kupima milima kwa mizani,
au vilima kwa usawa? 13 Ni nani aliyeelewa akili za Yahwe, au kumuelekeza yeye
kama mshauri? 14 Ni kutka kwa nani alipokea maelekezo milele? Nani alikufundisha
njia sahihi ya kufanya vitu, kumfundisha yeye maarifa, au kumuonyesha njia ya
ufahamu? 15 Tazama, Mataifa ni kama tone katika ndoo, na kama mavumbi kwenye
mizani; ona, na alipima kisiwa kama tundu. 16 Lebanoni sio mafuta ya kutosha,
wala wanyama pori wake hawatoshi kwa dhabihu ya kuteketezwa. 17 Mataifa
yote hayatochelezi mbele yake; wanachukuliwa na yeye kama hakuna kitu. 18 Ni
nanibasi utayemlingalisha na Mungu? Ni kwa sanamu ipi utakayomfananisha nayo?
19 Sanamu! ambayo fundi ameitupa: Mfua dhahabu ameka pamoja na mikufu bandi
ya fedha. 20 Kuafanya sadaka hii mtu atachagua kuni ambayo haiozi; anamtafuta
fundi mwenye ujuzi wa kutengeneza sanamu ambayo haitaanguka. 21 Je hamkujua?
Je hamjasikia? Je hamkuambiwa tokea mwanzo? Je hamkuelewa toka misingi ya
nchi? 22 Yeye ndiye aketie juu ya upeo wa macho ya nchi? na wenyeji wake ni
kama panzi mbele yake. Akijinyoosha nje ya mbingu ni kama pazia na kutawnya
nje kama hema la kuishi. 23 Anawapunguza viongozi kuwa si kitu na amewafanya
viongozi wa nchi kwa sio wenye umuhimu. 24 Tazama wamekuwa wagumu kuotesha;
tazama wamekuwa wagumu kupanda; imekuwa ni vigumu kuchukua mzizi katika
nchi, kabla ajapuliza juu yao, na wakanyauka, na upepo unawaondosha mbali kama
majani. 25 Ni nani tena utakayemfananisha na mimi, ni nani ninayefanan nae?"
amesema mtakatifu. 26 Tazama juu kwenye anga! Nani aliyeziumba nyota hizi zote?
Analileta nje jeshi na anawaita kwa majina yote. Kwa ukuu wa nguvu zake na kwa
uimara wa nguvu zake, hakuna hata mmoja atakayekosa. 27 Kwa nini unasema,
Yakobo, na kutangaza, Israeli, "Njia yangu imefichwa Yahwe asione, na Mungu wangu
hakuwekwa wazi kuhusiana na uthibitisho wangu"? 28 Je hakufahamu? Mungu wa

milele, Yahwe, Muumbaji wa miisho ya nchi, apatwi na uchovu wala hachoki; hakuna
mipaka katika ufahamu wake. [29] Anawapa nguvu waliochoka; na atawapa nguvu
mpya waliowadhaifu. [30] Hata vijana wadogo watapatwa na uchovu na kuchoka,
vijana wadogo watapata mashaka na kuanguka: [31] Lakini wale watakao mngojea
Yahwe watapewa nguvu mpya; na watapaa kwa mbawa kama malaika; watakimbia
wala hawatachoka; watatembea wala hawatazimia.

# 41

[1] ''Sikilizeni mbele yangu kwa ukimya, enyi mkao pwani; wacha mataifa yapate
nguvu kwa upya; waache waje karibu na kuzungumza; na tusogee karibu tujadili
mgogoro. [2] Nani aliyechochea juu mmoja kutoka mashariki, anamuita katika haki
yake kwenye huduma yake? Amemkabidhi mataifa juu yake ili amsaidie yeye
kuwaangamiza wafalme. Aliwajeuza kuwa mavumbi kwa neno lake, kama upepo
unaovuma kwenye mabua kwa upinde wake. [3] Aliwachukuwa wao na kuwapitisha
salama, katika njia nyepesi ambayo miguu yake imegusa shida. [4] Ni nani aliyeyafanya
na kukamilisha matendo haya? Ni nanialiyechagua kizazi kutoka mwanzo? Mimi,
Yahwe ni mwanzo na mwisho, mimi ndiye. [5] Visiwa vimeona na kuogopa; miisho
ya dunia yatetemeka; walikaribia n kuja. [6] Kila mmoja amsaidie jirani yake, na kila
mmoja asemezane na mwenzake, 'Kuwa mfariji; [7] Hivyo basi seremala anamfariji
mfua dhahabu, na yule anayefanya kazi kwa kutumia nyundo anamfariji anayefanya
kazi kwa chuma, akisema kwa msemo wa kurehemu, ''Ni mizuri; Naye ataupigilia
kwa makini misumari ili isipinduke. [8] Lakini wewe, Israeli mtumishi wangu, Yakobo
niliyekuchagua, mtoto wa Ibrahimu rafiki yangu, [9] wewe ambaye ninakurudisha
kutoka miisho ya nchi, na ambaye niliyekuita kutoka sehemu ya mbali, na kwako
niliyekuambia, 'Wewe ni mtumishi wangu,; 'Nimekuchagua wewe na sijakukataa.
[10] Usiogope maana mimi niko pamoja na wewe. Usiwe na wasiwasi, maana mimi ni
Mungu wako. Nitakutia nguvu, na nitakusaidia, wewe, na Nitakushika kwa mkono
wa haki yangu. [11] Tazama, watakuwa na aibu na hawataheshimiwa, wale wote
waliokuwa na hasira na wewe; watakuwa si kitu na watatokomea, wale watakao
kupinga wewe. [12] Utawatafuta na wala hautawapata wale wanaopingana na wewe;
wale wafanyao vita dhidi yako watakuwa kama si kitu, si kitu kabisa. [13] Maana
mimi Yahwe Mungu wako, nitawashika mkono wako wa kiume, nikikuambia wewe,
'Usiogope; Nitakusaidia wewe. [14] Usiogope, Yakobo wewe mdudu, na enyi watu
wa Israeli; Nitawasaidia''- hili ni tamko la Yahwe, Mkombozi wako, Mtakatifu
wa Israeli. [15] Tazama, ninakufanya wewe kuwa chombo kikali cha kuparulia
chenye makali pande mbili; utaparua milima na kuiponda; utafanya vilima kama
makapi. [16] Utawatawanya wao, na upepo utawabeba na kuwapeka mbali; upepo
utawatanya wao. Utashanglia katika Yahwe, utashangiliakatika mtakatifu wa Israeli
[17] Waliodhulumiwa na masikini wanatafuta maji, lakini hakuna kitu, ndimi zao
zimekauka kwa kiu; Mimi Yahwe, nitajibu maombi yao; Mimi Mungu wa Israeli,
sitawacha wao. [18] Nitatengeneza mikondo ya maji kushusha chini, na chemichem
katikati ya mabonde; nitalifanya jangwa kuwa kisima cha maji, na aridhi kavu
kuwa chemichem ya maji. [19] Katika jangwa nitapanda mierezi, mshita, mhadisi,
na mti wa mizeituni. Nitaotesha mberoshi katika uwazi wa jangwa, pamoja na
mbono nitapanda mberoshi kitika jangwa lililowazi. [20] Nitayafanya haya ili waweze
kuona, kutambua na kuelewa kwa pamoja, kwamba mkono wa Yahwe umetenda
haya, kama Mtakatifu wa Israeli aliyeliumba. [21] Wakilisha keshi yako, '' asema
Yahwe; ''wakilisha hoja zenu nzuri kwa sanamu yenu,'' asema Mfalme wa Yakobo.
[22] Waache walete hoja zao wenyewe; waache waje mbele na watutangazie sisi
nini kitakachotokea, ili tuweze kuelewa haya mambo vizuri. Tuawaache watupe

tamko mapema, ili tuweze kulitafakari na tuweze kujua n kwa jinsi gani litatimia.
23 Wajulishe kitu kuhusu baadaye, ili tujue kuwa ninyi ni miungu; fanya kitu kizuri
au kibaya, ambacho kitatutisha na kutushangaza. 24 Tazama sanamu zenu si kitu
na matendo yenu si kitu; aliyewachagua ni machukizo. 25 Nimemnyanyua mmoja
kutoka kaskazini, naye amekuja kutoka mawio ya jua nimemchagua yeye alitajae
jina langu, na atawakanyaga viongozi kama matope, kama mfinyanzi akanyagavyo
udongo. 26 Ni nani aliyetangaza hili tangu mwanzo, ili tuweze kujua? na kabla ya
mda, ili tuseme, ''Yuko sawasawa''? Kweli hakuna hata mmoja aliyekiri hili, ndio
hakuna hata mmoja aliyekusikia ukisema chochote. 27 Kwanza nilizungumza na
Sayuni, ''Tazama hapo walipo;'' Nimemtuma mhubiri Yerusalemu. 28 Nilipoangalia,
hakuna hata mmoja, hakuna hata miongoni mwao ambaye anaweza kutoa ushauri
mzuri, nani, lini nimulize, awezaye kunijibu neno. 29 Tazama, matendo yao si kitu;
sanamu zao za chuma zilizotupwa ni upepo na utupu.

# 42

1 Tazama, mtumishi wangu, niliyekushika; niliyekuchagua, kwake ninapata furaha.
Nimeiweka roho yangu juu yake; ataleta haki kwa mataifa. 2 Hatalia wala kupiga
kelele, wala sauti yake haitasikika mitaani. 3 Mwanzi ulioangamizwa hatauvunja,
na wala utambi unaowaka na kutoa mwanga hautaungua: atatekeleza haki kwa
uaminifu. 4 wala hatazimia wala kukata tamaa mpaka atakapoanzisha haki katika
nchi; na pwani inasubiria sheria yake. 5 Mungu Yahwe asema hivi—yeye aliyeziumba
mbingu na yeye zinyoosha nje, yeye aliyeiumba nchi na vitu vyote izalishavyo,
yeye aliyewapa punzi watu na wale waishio juu: 6 Mimi Yahwe nimekuita kwa
haki yangu na nitakushika kwa mkono wangu. Nitakutunza wewe, na nitakuweka
wewe kama agano kwa watu wangu, kama mwanga wa wayunani 7 Kuyafungua
macho ya vipofu, kuwatoa waliofungwa gerezani, kuwatoa wale walio gizani kutoka
kwenye nyumba iliyofungiwa. 8 Mimi ni Yahwe, Hilo ndilo jina langu; na utukufu
wangu sitashiriana na mtu mwingine wala sifa zangu sitashirkiana na sanamu
ya kuchonga. 9 Tazama, mambo ya nyuma yamekuja na kupita, sasa ninakaribia
kutangaza mambo mapya. Kabla hayajaanza kutokea nitawambia kuhusu wao.''
10 Mwimbieni Yahwe wimbo mpya, na sifa zake kutoka mwisho wa nchi; wewe
ushukae chini kwenye bahari, na vyote vilivyomo ndani yake, waishio pwani na
wale wanaoishi huko. 11 Wacha jangwa na miji ilie, vijiji anavyoishi na Kaderi, lia
kwa furaha! waache wenyeji wa Sela waimbe; waache wapige kelele juu ya kilele
cha mlima. 12 waache wamtukuze Yahwe na kutangaza sifa zake katika aridhi ya
pwani. 13 Yahwe atatoka nje kama shujaa; kama mtu wa vita ataichochea bidii yake.
Atapiga kelele, ndio, atalia kw kishindo katika vita yake; atawaonyesha adui zake
nguvu zake. 14 Nimenyamaza kimyi kwa mda mrefu; bado nimendelea kujizuia
mimi mwenyewe; Nitalia kama mwanamke anayetaka kuzaa; nitatweta na kuugua.
15 Nitaiharibu milima na vilima na kukausha uoto wake wa asili; nitajeuza mito kuwa
visiwa na nitakausha matindiga. 16 Nitawaleta vipofu kwa njia wasioijua; katika
njia wasiyoijua Nitawapitisha wao. Nitaligeuza giza kuwa mwanga mbele yao, na
kupanyoosha mahali palipopotoka. Mambo yote haya nitayafanya, na sitaachana
na wao. 17 Watageuka nyuma, wataabishwa sana, wale wote wanaoiamini sanamu
ya kuchonga, wanaosema na kuziambia sanamu za chuma, ''Nyinyi ni miungu
wetu.'' 18 Sikilizeni ewe kiziwi; tazama, ewe kipofu, ili uweze kuona. 19 aliye
kipofu ila mtumishi wangu? au kiziwi ni kama mjumbe niliyemtuma? Ni nani
aliye kipofu kama mpenzi wangu wa agano, au kipofu kama mtumishi wa Yahwe?
20 Mmeona mambo mengi, lakini hamuelewi; masikio yamefunguka, lakini hakuna
anayesikia. 21 Itampendeza Yahwe kuisifu haki yake na kuitukuza sheria yake.

22 Lakini watu hawa ni wale waliokamtw na kutekwa; wote wamenaswa kwenye
mashimo; wafungwa wote wamewekwa gerezani; wamekuwa mateka na hakuna
hata mmoja wa kuwaokoa wao, hakuna asemaye, warudisheni.'' 23 Ni nani miongoni
mwenu atalisikiliza hili? nani atayasikia na ni nani atasikia wakati ujao? 24 Ni nani
aliyemtoa Yakobo kwa majambazi, na Israeli kwa wanyang'anyi? Je hakuwa Yahwe,
dhidi ya wale waliotenda dhambi, waliokataa kutembea katika njia zako na wale
waliokataa kusheshimu sheria yako. 25 Hivyo basi humwaga asira yake kali nje dhidi
yao, kwa uharibifu wa vita. Iliwaka kuwazunguka wao, hata hawakujua hilo, lakini
hawakuyachukulia hayo moyoni mwao.

# 43

1 Lakini sasa haya ndio Yahwe asemayo, yeye aliyekuumba ewe, Yakobo, na yeye
aliyekuumba ewe, Israeli: ''Usiogope, kwa maana nimekukomboa wewe; nmeikuita
kwa jina lako, wewe ni wangu. 2 Utakapopita katika maji, Nitakuwa pamoja na
wewe; na katika mito, hayatakuzuru wewe. Utakapotembea katika moto hautaungua,
na moto hautakuharibu wewe. 3 Maana mimi Yahwe Mungu wako, Mtakatifu
wa Israeli Mkombozi wenu. Nimewapa Misri kama fidia yenu, Ethiopia na Seba
watabadilishana kwako. 4 Kwa maana ulikuwa wa thamani na maalumu katika
macho yangu, Ninakupenda; kwa sababu hiyo Nitatoa watu kwa ajili yako, na
watu wengine kwa ajili ya maisha yako. 5 Usiogope, maana Mimi niko pamoja na
wewe; Nitawarudisha watoto wako kutoka mashariki, na kuwakusanya nyie kutoka
magharibi. 6 Nitasema na kaskazini, 'Wakabidhini wao; na kwa kusini, Usiangalie
ya nyuma; Leteni vijana wangu kutoka mbali na binti zangu kutoka vijiji vya
mikoani katika nchi, 7 yeyote aitwe kw jina langu, niliyemuumba kwa utukufu wangu
mwenyewe, Niliyemuumba, ndio, Mimi niliyemfanya. 8 Waleteni nje watu ambao
ni vipofu, hata kama wana macho, na viziwi, hata kama wana masikio. 9 Mataifa
yote yatakusanyika kwa pamoja na watu watakusanyika. Ni nani miongoni mwenu
atakaye tamka na kutangaza kutumia mambo ya mwanzo? Waache walete mashahidi
kuwashuhudia wao kama wako sahihi, waache wasikilize na kuthibitisha, 'kama
ni kweli'. 10 Ninyi ni mashahidi wangu, ametangaza Yahwe, ''na watumishi wangu
niliowachagua, ili uweze kujua na kuniamini mimi, na kuelewa kwamba mimi ndiye.
Kabla yangu hapana mungu mwingine aliyeumbwa, na wala hatatoke baada yangu.
11 Mimi, Mimi Yahwe, na hakuna Mkombozi zaidi yangu. 12 Nimetangaza, nimeokoa,
na kutangaza, na hakuna Mungu mwingine miongoni mwenu, Ninyi ni mashahidi
wangu asema Yahwe, ''Mimi ni Mungu. 13 Kuanzia leo na kuendelea mimi ndiye,
na hakuna hata mmoja atakayewakomboa kwenye mkono wangu. Nitafanya, na
nani awezae kunizuia?'' 14 Yahwe asema hivi, Mkombozi wenu, yeye Mtakatifu wa
Israeli: ''Kwa niaba yenu nimemtuma mjumbe kwenda Babeli na kuwaongoza wao
wote chini kama watuhumiwa, kubadilisha kelele za furaha za watu wa Babeli' kuwa
wimbo wa maombolezo. 15 Mimi ni Yahwe, niliye Mtakatifu, Muumbaji wa Israeli,
Mfalme wenu. 16 Yahwe asema hivi, Ni nani aliyefungua njia katika bahari, na njia
katika maji yenye nguvu, 17 ni nani anayeongoza gari na farasi, majeshi na jeshi
kuu. Walianguka chini kwa pamoja; hawakunyanyuka tena; wamezimwa, kama
utambi unaoungua. 18 Msifikirie hayo mambo yaliyopita, wala kuyafikiria mambo ya
zamani. 19 Tazama ninakaribia kufanya mambo mapya; sasa yanakaribia kutokea;
Je humyajui haya? Nitafanya njia jangani na na mikondo ya maji katika jangwa
20 Wanyama pori wa shambani wataniheshimu mimi, Mbweha na mbuni, kwa sababu
ninatoa maji jangwani, na mito jangwani, ili watu wangu niliowachuga wapate
kunjwa, 21 Watu hawa niliowaumba mwenyewe, kwamba wahesabu tena sifa zangu.
22 Lakini hamjanita mimi, Yakobo; umechoka na mimi, Israeli. 23 Haujaniletea hata

kondoo wako kama sadaka ya kuteketeza; na wala haujaniheshimu mimi kwa sadaka
yako Sijakutumisha wewe kwa sadaka ya mazao, wala sijawachosha kwa sadaka yenu
ya ubani. 24 Hamkuninunulia mimi manukato mazuri kwa fedha, hakumwagia mimi
mafuta ya sadaka zenu; Lakini mnanichosha mimi na dhambi zenu na mnanichosha
mimi kwa matendo yenu mabaya. 25 Mimi, ndio, Mimi, ndiye niliyafaye maovu yenu
kwa niaba yangu mmi mwenyewe; na Sitawaita na kuwakumbusha dhambi zenu
tena. 26 Nikumbusheni mimi kilichotokea. Njooni tusemezane pamoja; leta hoja zako,
ili kusudi uthibitishe kuwa hauna hatia. 27 Baba yako wa kwanza alitenda dhambi,
na viongozi wenu walitenda dhambi dhidi yangu. 28 Hivyo basi Nitawatia unajisi
viongozi watakatifu; Nitamkabidhi Yakobo kuwaharibu kabisa, na Israeli kulaani
udhalilishaji.

# 44

1 Sasa, sikiliza, Yakobo mtumishi wangu, na Isreli, Niliyekuchagua: 2 Yahwe asema
hivi, yeye aliyekufanya na kukuumba wewe katika tumbo na yeye aliye kusadia
wewe: Usiogope, Yakobo mtumishi wangu; na wewe Yeshuruni, niliyekuchagua.
3 Maana nitashusha mvua kwenye aridhi yenye kiu, na mikondo ya maji kwenye
ardhi kavu; Nitashusha roho yangu kwa watoto wako, na baraka zangu kwa watoto
wako. 4 Watakuwa miongoni mwa nyasi, kama mti pembeni ya mkondo wa maji.
5 Mmoja atasema, 'Mimi ni wa Yahwe; na mwingine ataita jina la Yakobo, na
mwingine ataandika kwenye mkono wake 'Mimi ni wa Yahwe, na kujiita mwenyewe
kwa jina la Israeli.'' 6 Yahwe asema hivi—Mfalme wa Israeli na Mkombozi wake,
Yahwe wa majeshi: ''Mimi ni mwanzo na ni mwisho; na hakuna mungu ila mimi.
7 Ni nani aliye kama mimi? Na atangaze na anielezee matukio yaliyotokea tangu
nilipoanzisha watu wangu wa kale, na waache watangaze matukio yajayo. 8 Usiogope
wala usifadhaike. Je si mimi niliyekutangazia toka zamani, na nikatangaza? ninyi
ni mashaidi wangu: Je kuna Mungu mwingine zaidi yangu? Hakuna Mwamba
mwingine zaidi yangu; Ninajua hakuna.'' 9 Mitindo yote ya sanamu si kitu; vitu
wanavyo vifurahia ndani havina maana; mashahidi wake hawawezi kuona au kujua
chochote, na watapatwa katika aibu. 10 Ni nani atengenezae miungu au sanamu
zisizo na maana? 11 Tazama, washirika wote watapatwa na aibu; mafundi ni watu
tu. waache washikilie msimamao wao kwa pamoja; wataogopa na kuhaibishwa.
12 Mhunzi anafanya kazi kwa vyombo vyake, kutengeneza, kufanya kazi kwenye
makaa ya mawe. Hurekebisha kwa kutumia nyundo na hufanya kazi kwa mkono
wake wenye nguvu. Hupata njaa, na nguvu zake humuishia; Hajanywa maji na
huzimia. 13 Seremala hupima mbao kwa kamba na kuiweka alama kwa kitu kikali.
Huichonga kwa vyombo vyake na kuweka alama kwa kutumia dira. Huichonga
baada ya sanamu ya mtu, kama mtu anyevutia, ili iweze kukaa ndani ya nyumba.
14 Huikata chini mierezi, huchagua miti ya miseprasi au miti ya mialoni. Huchukua
mti yeye mwenyewe katika msitu. huotesha mvinje na mvua huifanya ikue. 15 Basi
mtu hutumia kwa moto na kujipatia joto. Ndio, huwasha moto kuwooka mkate.
Halafu hutengeneza miungu ili ausujudie; 16 Huchoma sehemu ya kuni kwa moto,
na huchoma nyama yake juu yake. hula na kushiba. huota moto na kusema, ''Ah,
Nimepata joto, nimeouna moto.'' 17 Kwa kutumia mbao hutengeneza miungu, sanamu
yake; huisujudu na kuhieshimu, huipa sifa na kusema, ''Niokoe mimi, maana wewe
ni mungu wangu.'' 18 Hawajui, wala hawaelewi, maana macho yao yamepofuka na
hawaoni, na mioyo yao haiwezi kufahamu. 19 Hakuna anayefikiria, wala kuelewa
na kusema, ''Nimechoma sehemu ya mbao kwenye moto; na pia nimewooka mkate
kwa kutumia makaa yake. Nimechoma nyama kwa makaa yake nikala. Sasa Je
ninaweza kutengeneza kitu kinachochukiza kwa ajili ya kuabudia kwa sehemu ya

mbao iliyobakia? Je ninaweza kusujudia sanamu ya mbao?'' 20 Ni kama anayejilisha
majivu; moyo wke mdanganyifu unampoteza yeye. Huwezi kujiokoa mwenyewe,
wala hawezi kusema, ''Hiki kitu katika mkono wangu wa kulia sio mungu wa
kweli.'' 21 Fikiria kuhusu vitu hivi, Yakobo na Israeli, maana wewe ni mtumishi
wangu: Nimekuumba wewe; wewe ni mtumishi wangu: 22 Nimeyafuta makosa
yako, kama wingu zito, matendo yako mabaya, na wingu, ni kama dhambi zako;
maana nimekukomboa wewe. 23 Imba, enyi mbingu, maana Yahwe ameyafanya
haya; piga kelele enyi mkaao katika nchi. Pazeni sauti enyi mlima milima, enyi
misitu yenye miti ndani yake, ewe mlima, ewe msitu wenye kila aina ya mti ndani
yak,; Maana Yahwe amemkomboa Yakobo, na nitakuonyesha utukufu wake katika
Israeli. 24 Yahwe asema hivi, Mkombozi wako, yeye aliyekuumba wewe kutoka
tumboni: ''Mimi ni Yahwe, niliyefanya kila kitu, mimi mwenyewe nizinyooshae
mbigu, mimi peke niitngenezae nchi. 25 Mimi niliyezikata dalili za waongo na
kuwaabisha wanaosoma dalili zake; Mimi niliyezigeuza busara za wenye hekima
na kujeuza ushauri wao kuwa ujinga. 26 Mimi, Yahwe, niliyethibitisha maneno ya
mtumishi wake na kuutimiza utabiri wa mjumbe wake. Aliyezungumza kuhusu
Yerusalemu, 'Atakuwa mwenyeji; na katika mji wa Yuda, 'Watatengeneza tena, na
nitapatengeneza palipoharibika; 27 awezae kusema kwa bahari kubwa, 'Kauka,' na
yanakauka mda huo.' 28 Yahwe ndiye amwambiye Koreshi, 'Ni mchungaji wangu,
atafanya kila nilitakalo; atatoa amri kuhusu Yerusalemu, 'Utajengwa kwa upya, 'na
kuhusu Hekalu, 'Basi na msingi wake uanzwe kuwekwa.''

# 45

1 Yahwe asema hivi kwa mapakwa mafuta, kwa Koreshi, niliyemshika kwa
mkono wa kuume, illi niweze kuangamiza mataifa mbele yake, kuwalinda wafalme,
kufunguo milango mbele yao, ili lango liwe wazi: 2 ''Nitakwenda mbele yako na
kusawazisha milima; nitavunjavunja vipandevivande milango ya shaba na kukuta
vipandevipande nguzo za chuma, 3 Nitakupa hazina iliyo gizani na utajiri uliofichwa
mbali, ili ujue kwamba ni mimi Yahwe, niliyekuita kwa jina lako, Mimi, Mungu wa
Israeli. 4 Kwa niaba ya Jakobo mtumishi wangu, na Israeli chaguo langu, Nimekuita
wewe kwa jina lako: nimekupa heshima iliyotukuka, jabo hakunijua mimi. 5 Mimi
ni Yahwe na hapana mwingine; hakuna Mungu ila mimi. Nitakuimarisha katika
vita, japo hamkunifamu mimi; 6 kwamba watu wajue kutoka mapambazuko ya
jua, na kutoka magharibi, kwamba hakuna mungu mwngine ila mimi: Mimi ni
Yahwe, na hakuna mwingine. 7 Nimefanya mwanga na nimeumba giza; Ninanateta
amani na ninaumba majanga; Mimi Yahwe, nifanyae haya yote. 8 Enyi mbingu,
nyesha kutoka juu! Acha anga lishushe chini haki, na acha nchi inyonje haki, ili
wokovu uweze kuchipukia juu, na haki kutawanyika kwa pamoja. Mimi Yahwe
nimewumba wote kwa pamoja. 9 Ole kwa yeyote anayesema kwa yule aliyemfanya
yeye, kwake yeye ni kama chungu cha udongo miongoni mwa vyingu vya udongo
katika aridhi! Je udongo umwambia mfinyanzi, 'Unatengeneza nini? au ' Kazi yako
haina kitu cha kushika? 10 Ole wake asemae kwa baba, 'Unanizaa nini? au kwa
mwanamke, 'unanizaa mimi nin?' 11 Yahwe asema hivi, yeye aliye Mtakatifu wa
Israeli, muumbaji wake: 'Kwa nini unauliza swali kuhusu nini nitakacho kifanya
kwa watoto wangu? Je unaweza kuniambia kuuhusiana na kazi ya mikono yangu?
12 Nimeifanya nchi na kuumba mtu juu yake. Ni mkono yangu mimi nilioinyoosha
ju ya mbingu, na nikazimuru nyota zote kutokea. 13 Nimemuinua Keroshi juu katika
haki yangu, na nitalainisha njia zake zote. Ataujenga mji wangu kwa upya; atawachia
walioko uhamishoni kurudi nyumbani kwao, na so kwa pesa wala kwa rushwa,''
asema Yahwe wa majeshi. 14 Yahwe asema hivi, mapato ya Misri na bidhaa ya

Ethiopia pamoja na Waseba jamii ya watu werefu, tatawaleta kwenu. Watakuwa wa kwenu. Watafuata baada yenu, watakuja na minyororo. Watakuinamia chini na kukuomba huku wakisema, 'Hakika Mungu yuko pamoja na wewe na hakuna
mwingine ila yeye.'' 15 Hakika mna Mungu aliyejifisha ndani yenu, Mungu wa
Israeli, Mkombozi. 16 Wote wataabishwa na kuzaraliwa kwa pamoja; wale wachongao
sanamu watatembea katika udhalilishaji. 17 Lakini Israeli itakombolewa na Yahwe
kawa wokovu wa milele; na wala hautaabika tena au kudhalilishwa. 18 Yahwe asem
hivi, nani aliyeziumba mbingu, Mungu wa kweli ndiye aliyeiumbwa nchi na kuifaya, ndiye aliyeianzisha nchi. Aliiumba yeye, sio kama taka, aliimba ili pawe na wenyeji:
''mimi ni Yahwe, na hakuna mwingine. 19 Sijaongea katika siri, katika maeneo ya siri;
Sijauambia ukoo wa Daudi, 'Nitafute bure! Mimi ni Yahwe ninayezungumza ukweli;
Ninatangaza vitu vilivyo vya kweli. 20 Jikusanjeni wenyewe na mje! kusanyikeni
kwa pamoja, enyi wakimbizi kutoka miongoni mwa mataifa! Hawana maarifa, wale
wanaobeba sanamu ya kuchonga na kuiomba miungu asiyewasidia. 21 Sogeeni karibu
na mnitangazie mimi, leteni ushahidi! waache walete mashauri kwa pamoja. Ni nani aliyewaonyesha haya kutoka zamani? Ni nani aliyetangaza? Je sikuwa mimi, Yahwe? na hakuna Mungu mwingine ila mimi, Mungu mwenye haki; na mkombozi; hakuna
mwingine zaidi yake. 22 Nijeukieni mimi, na mkaokolewe, miisho yote ya nchi;
Maana mimi ni Mungu, na hakuna mwingine. Mimi mwenyewe ninaapa, ninaongea
katika haki yangu, na sitarudi nyuma: 23 'kwangu kila goti litapigwa, na kila ulimi
utakiri. 24 Wataniambia mimi, Ni katika Yahwe peke yake kuna wokovu na nguvu.''
wataaibika wale wote wenye hasira na Mungu. 25 Katika Yahwe makabila yote ya
Israeli yataalalishwa; watachukua kiburi katika yeye.

# 46

1 Beli huaguka chini, Nebo husujudu; miungu yao imebebwa na wanyama
na mzigo wa mnyama. Sanamu hizi mlizobeba ni mzigo mzito kwa wanyama
kuchoka. 2 Kwa pamoja wanashuka chini; hawawezi kuziokoa sanamu zao, na
wao wenyewe wameenda uhamishoni. 3 Nisikilizeni mimi, nyumba ya Yakobo,
wote mliobaki kwenye nyumba ya Israeli mliochukuliwa na mimi kutoka kabla
amjazaliwa, mlichukuliwa mkiwa tumboni. 4 Hata kwa njie wazee Mimi ndiye,
mpaka mmeshapata mvi nitawachukua. Nimewaumba ninyi na nitawabeba ninyi;
Nitwachukua nyie na nitawakomboa nyie. 5 Je utanifananisha mimi na nani? na
mimi nimefanana na nani, ili utulinganishe? 6 Watu humwaga dhahabu kutoka
kwenye mabegi yao na uzito wa fedha kwenye uzani. Humuajiri mfua dhahabu, na
hutengeneza kuwa dhahabu; na huinama chini na kuzisuju. 7 Wanazinyanyua juu ya
mabega yao na kuzibeba; wanaziweka katika sehemu yake, na itasimama katika eneo lake na alitasogea kutoka pale, hulilia, lakini haiwezi kujibu wala kumuokoa yeyote
kwenye matatizo. 8 Tafakari kuhusu hivi vitu; katu usivipuuzie, enyi waasi! 9 Tafakari
kuhusu vitu vya awali, nyakati zile zilizopita, Maana mimi ni Mungu, na hakuna
mwingine, Mimi ni Mungu na hakuna kama mimi. 10 Mimi ninatangaza mwisho
kutoka mwanzo, na kabla ya kitu ambacho hakijatokea; Ninasema, ''Mpango wangu
utatokea na nitafanya kama ninavyotamani.'' 11 Nitamuita ndege wa mawindo kutoka
mashariki, Mtu ambaye ni chaguo langu kutoka nchi ya mbali; Ndio nimesema; na pia
nitayatimiza haya, nimekusudia, na pia nitafanya hivyo. 12 Nisikilize mimi, enyi watu
makaidi, ambao mko mbali na kutenda mema. 13 Ninaileta haki yangu karibu; na
wala sio mbali, na wokovu wangu hausubiri; na nitatoa wokovu wangu kwa Sayuni
na uzuri wangu kwa Israeli.

# 47

1 Njoo chini na ukae kwenye mavumbi, binti bikira wa Babeli; kaa juu ya aridhi
pasipo enzi, ewe binti wa Wakaldayo. Hautaitwa tena mpenda anasa na maisha ya
anasa. 2 Chukua jiwe la kusagia na usage unga; ondoa pazia lako, ondoa mavazi
yako, ondoa viatu miguuni, na vuka mkondo wa maji. 3 Uchi wako utafunuliwa,
ndio, na aibu yako itaonekana; Nitachukua kizazi na sitamuacha mtu, 4 Mkombozi,
Yahwe wa majeshi ndilo jina lake, Mtakatifu wa Israeli. 5 Kaa kimya na nenda
katika giza, ewe binti wa Wakaldoyo; maana hautaitwa tena malikia wa falme.
6 Nilikuwa na hasira na watu wangu; Nimeunajisi urithi wangu na kuwakabidhi
nyie katika mkono wenu, lakini hamkuomyesha huruma; umeweka nira kubwa kwa
wazee. 7 Umesema, ''Nitaongoza daima kama malikia huru.'' Haukuvichukua vitu
hivi katika moyo, wala hakutafakari jinsi hivi vitu vitakavyojeuka. 8 Hivyo sasa
sikiliza hili, Ewe upendae anasa na kukaa salama; ewe usemae katika moyo wako,
'Ninaishi, na hakuna mwingine kama mimi; Sitakaa kama mjane wala sitazoea kufiwa
na watoto. 9 ''Lakini vitu hivi vitakuja kwako siku moja katika kipindi cha siku
moja; kwa nguvu za kutosha yatakuja kwako, japo uchawi wako na dua zako na
hirizi. 10 Umeweka imani katika mapungufu yako; na kusema, ''Hakuna anayeniona
mimi''; hekima na maarifa yako yanakupoteza, lakini unasema katika moyo wako,
''Nipo na hakuna hata mmoja kama mimi.'' 11 Maafa yatakuzidi wewe; hautaweza
kuyaondoa kwa dua zako mwenyewe. Uharibifu utakuwa juu yako; hautaweza
kuukata. Maafa yatakuangamiza ghafla, kabla haujajua kitu. 12 Endeleni kutoa
uganga wako na wachawi wengi ambao mlioaminishwa kusoma toka utotoni mwao;
labda utafanikiwa, labda utayashinda maafa. 13 Umejaribu sana kwa kushauriwa
sana; waache hao watu wasimame na kukuokoa wewe- wale wanaoangalia mbingu
na wanoangalia nyota, wale wanotangaza mwenzi mpya- waache wawaokoe nyie
kutoka kwenye yaliyowapata. 14 Tazama, watakuwa kama mabua. Moto utayachoma
juu. Hayataweza kujisaidia yenyewe kutoka kwenye mkono wa moto. Hakuna makaa
kuwapa joto wao na hakuna moto uliowekwa pembeni kwa ajili yao! 15 Hivi ndio
wamekuwa kwako, wale unaofanya nao kazi, na unauza na kununua na wao toka
ulipo kuwa mdogo, na wale wanaendelea kufanya mambo yao ya kijinga; na unapolia
kuhitaji msaada, hakuna hata mmjoa ambaye atakukomboa wewe.''

# 48

1 Sikiliza hili, nyumba ya Jakobo, mlioitwa kwa jina la Israeli, na mmetoka katika
mbegu ya Yuda; yeye akirie kwa jina la Yahwe na kumuhusisha Mungu wa Israeli,
lakini sio kweli wala kwa namna ya haki. 2 Maana wanajiita wenyewewatu wa
mji mtakatifu na kumuamini Mungu wa Israeli; Yahwe wa majeshi ndilo jina lake.
3 ''Nimetangaza vitu kutoka siku nyingi; Wamekuja nje kutoka mdomoni mwangu, na
nimewafanya wajulikane; halafu gafla nimewafanyia, na yakatimia. 4 Kwa sababu
nilijua kwamba wewe ni mkaiidi, misuli ya shingo yako ni kama ya chuma, na paji
la uso ni kama shaba, 5 Hivyo basi nilitangaza vitu hivi kabla havijatokeo hivyo,
nilikujulisha wewe, 'Sanamu yangu imefanya haya au sanamu yangu ya kuchonga
na sanamu yangu ya kuyeyusha, yamekwishisha vitu. 6 Umesikia kuhusu mambo
haya; angalia ushahidi wote; na wewe, Je hautakubali kwamba ninacho kisema ni cha
kweli? Kuanzia sasa na kuendelea Nitawaonyesha vitu vipya, mambo yaliyofichika
ambayo hamkuyajua. 7 Sasa, na sio yaliyopita, yamekuwa sasa, na kabla ya leo
hamkusikia kuhusu wao, hivyo hautaweza kusema, 'Ndio, nilijua kuhusu wao.'
8 Haukusikia; haukuelewa; haya mambo hayakufuniliwa katika masikio kabla ya.
Maana nilijua kwamba umekuwa mdanganyifu, na kwamba umekuwa muasi kutoka
kuzaliwa. 9 Kwa niaba ya jina langu nitahairisha asira yangu, na kwa heshima yangu

nitajizuia kutokumuharibu yeye. 10 Tazama, Mimi niliwaandaa ninyi, lakini sio kama
fedha; Nimekusafisha wewe katika tanuru la mateso. 11 Kwa niaba yangu, kwa niaba
yangu nitafanya; maana ni kwa jinsi gani niruhusu jina langu lisiheshimike? Sitampa
utukufu wangu mtu yeyote. 12 Nisikilize mimi, Yakobo, na Israeli niliyekuita: Mimi
ndiye; Mimi ni wa kwanza, na pia wa mwisho. 13 Ndio, mkono wangu umeweka
msingi wa nchi, na mkono wangu wa kuume ulizitawanya mbingu, zimesimama juu
kwa pamoja. 14 Jikusanyeni wenyewe, nyinyi nyote, na sikilizeni; ni nani miongoni
mwenu atangazaye mambo haya? Yahwe atakamilisha lengo lake dhidi ya Babeli.
Atachukua mapenzi ya Yahwe dhidi ya wa Wakaldayo. 15 Mimi, nimezungumza, ndio,
nimemchagua yeye, nimemleta yeye, na yeye atafanikiwa. 16 Sogea karibu na mimi,
sikiliza hili; kutoka mwanzo sikuzungumza katika siri; lakini ilipotokea, Mimi niko
hapa; na sasa Bwana Mungu amenituma mimi, na Roho wake.'' 17 Yahwe asema
hivi, Mkombozi wenu, Mtakatifu wa Israeli anasema, ''Mimi ni Yahwe Mungu wenu,
ninayewafundisha juu ya kufanikiwa, ninayewaonyesha njia mtakayoiptia. 18 Ikiwa
kama mtaheshimu amri zangu! Hivyo amani na maendeleo yatatiririka kama mto,
na wokovu wenu ni kama mawimbi kwenye bahari. 19 Watoto wako watakuwa wengi
kama mchanga, na watoto kutoka kwenye tombo zenu watakuwa wengi kama nafaka
kwenye mchanga; majina yao hayataondolewa wala kufutwa mbele yangu. 20 Tokeni
nje ya Babeli! wakimbieni Wakaldayo! kwa sauti ya kupiga kelele tangaza kwamba!
hakikisha hili linajulikana, hakikisha hili linafika mpaka miisho ya nchi! sema 'Yahwe
amemkomboa Yakobo mtumishi wake. 21 Hawakupatwa na kiu alipowaongoza katika
jangwa, alifanya maji kutokea kwenye mwamba kwa ajili yao; aliugawa na kufungua
mwamba, na maji yakatoka nje. 22 Hakuna amani kwa watenda makosa- amesema
Yahwe.''

# 49

1 Nisikilize mimi, enyi mkao pwani! na kuwa makini, enyi watu mkao mbali.
Yahwe amenita mimi kutoka kuzaliwa kwa jina, mama yangu aliponileta duniani.
2 Amefanya mdomo wangu kuwa kama upanga mkali; amenificha mimi katika kivuli
cha mkono wake; amenifanya mimi kuwa mshale unaong'aa; katika podo yake
amenificha mimi. 3 Amesema na mimi, ''Wewe ni mtumishi wangu, Israeli, kupitia
yeye nitaonyesha utukufu wangu.'' 4 Lakini nilimjibu, ''Japo nilifikiria nilifanya kazi
bure, nimetumia nguvu zangu bure, ikiwa haki yangu iko pamoja na Yahwe, na
zawadi yangu iko kwa Mungu wangu. 5 Na sasa Yahwe asema hivi, yeye aliyeniumba
mimi toka kuzaliwa na kuwa mtumishi wake, kumrejesha Yakobo tena kwake
mwenyewe, na Israeli wakusanyike kwake. Mimi ninaheshimika katika macho ya
Yahwe, na Mungu wangu amekuwa nguvu zangu. 6 Asema hivi, ''Ni kitu kidogo sana
kwa wewe kuwa mtumishi wangu ili kuanzisha ukoo wa Yakobo, na kuwarejesha
wanaoishi Israeli. Nitakufanya wewe kuwa mwanga kwa Wayunani, ili uwe wokovu
wangu katika mipaka ya nchi. 7 Yahwe asema hivi, Mkombozi wa Israeli, Mtatakatifu
wao, kwa yeye ambae maisha yake yamedharauliwa, kuchukiwa na mataifa, na
mtumwa wa viongozi, ''Mfalme atakuona wewe na nyanyuka, na wakuu watakuona
wewe na inama chini, kwa sababu ya Yahwe ambae ni mwaminifu, hata mtakatifu
wa Israeli, aliyewachagua ninyi.'' 8 Yahwe asema hivi, ''Kwa mda huu nimeamua
kuwaonyesha neema yangu na nitawajibu ninyi, na siku ya wokovu nitawasaidi
ninyi; Nitakulinda wewe; na nitawapa kama agano kwa watu, kuitengeneza tena
nchi, kuwarihtisha urithi uliokuwa na ukiwa. 9 Utasema kwa wafungwa, 'Tokeni nje;
kwa wale mlio katika giza gerezani, 'Jionyeshe mwenyewe. 'Watachunga pembeni
ya barabara, na juu ya miteremko ya wazi yatakuwa malisho yake. 10 Hawatasikia
njaa wala kiu; wala joto au jua halitawaunguza, kwa yeye mwenye huruma juu

yao atawaongoza wao; atawaongoza wao kwenye mikondo ya maji. 11 Na nitafanya
milima yote kuwa barabara, na kufanya njia za juu kuwa sawa" 12 Tazama, haya
yatatoka kutoka mbali, baadhi kutoka kaskazini na magharibi; na wengine kutoka
nchi ya Sinimi. 13 Imba, ewe mbingu, na uwe na furaha, ewe nchi pazeni sauti
ya kuimmba enyi milima! maana Yahwe anawafariji watu wake, na watakuwa na
huruma kwa wale wanoteseka. 14 Lakin Sayuni asema, Yahwe ameniacha mimi,
na Bwana amenisahau mimi." 15 "Je mwanamke anaweza kumsahau mtoto wake,
aliyemnyonyesha, hivyo hana huruma na mtoto aliye mzaa? ndio, hawakusahau,
lakini siwezi kukusahau wewe. 16 Tazama, nimeliandika jina lako kwenye kiganja
cha mkono wangu; Kuta zako zinaendelea kuwa mbele yangu. 17 Watoto wangu
wamerudi haraka, wakati wale wanowaangaimiza nyie wameenda mbali. 18 Tazama
karibu na uone, wote wamekusanyika na wanakuja kwako. Nitahakikisha kama
ninaishi- hili ni tamko la Yahwe- hakika mtavivaaa kama kama kijiti; utajifungia kama
bibi harusi. 19 Japo umeharibiwa na kuwa na ukiwa, nchi iliyoharibiwa, sasa itakuwa
ndogo sana kwa wenyeji, na wale wanao waliokumeza watakuwa mbali, 20 Watoto
watakaozaliwa katika kipindi cha msiba watasema mkiwa mnawasikiliza, 'Sehemu
hii ni duni kwetu, tengeneza chumba kwa ajili yetu, ili tuweze kuishi hapa. 21 Halafu
utajiuliza mwenyewe, ni nani aliyewazaa watu hawa kwangu? Mimi nilifiwa na ni
tasa, niliyefungwa na kupewa talaka. Ni nani aliyewalea hawa watoto? Tazama,
niliachiwa yote mimi mwenyewe; Je haya yametoka wapi?" 22 Yahwe asema hivi,
"Tazama, nitanyanyua mkono wangu juu ya mataifa; Nitanyanyua bendera yangu
ya ishara kwa watu. Watawaleta watoto wako kwenye mikono yao na watawabeba
binti zako juu ya mabega yao. 23 Wafalme watakuwa baba zako wa kambo, na malikia
watakuwa wafanyakazi wa ndani; watakuinamia chini wewe kw uso wao kwa nchi
na kukung'uta mavumbi ya miguu yenu; wale wanonisubiri mimi hawataabika." 24 Je
mateka wanaweza kuchukuliwa kwa shujaa, au wafungwa kukombolewa kutoka kwa
mkali? 25 Lakini Yahwe asema hivi, "Wafungwa watachukuliwa kutoka kwa shujaa,
na maeteka watakombolewa; maana utampinga adui yako na kuwakomboa watoto
wako. 26 Na nitawalisha wanowaonea kwa mwili wao wenyewe; na watalewa kwa
damu zao wenyewe, kama iliyo mvinyo; na watu wote watajua kwamba Mimi Yahwe,
ni Mokozi wenu na Mkombozi wenu, yeye aliyemkuu wa Isareli.

# 50

1 Yahwe asema hivi, "Kiko wapi cheti cha talaka ambacho nimempa tataka mama
yako? na kwa nani niliowauza mimi? Tazama, umewauza kwa sababu ya dhambi
zako, na kwa sababu ya uasi wako, na mama yako amepelekwa mbali. 2 Kwa
nini nimekuja maana hakuna mtu pale? Kwa nini nimeita lakini hakuna aliyejibu?
Je mkono wangu ni mfupi kukufidia wewe? Je hakuna nguvu katika ukombozi
wngu kwako? Tazama, maonyo yangu, nimeikausha bahari; nimeufanya mto kuwa
jangwa; samaki wake wamekufa na kuoza kwa kukosa maji. 3 Nimelivisha giza; na
ku kwa ngfunika nguo za magunia." 4 Bwana Yahwe amenipa mimi lugha kama
wale wanayofundishwa, ili kwamba nizungumze maneno ya kudumisha kwa yeye
aliyechoka; huniamsha mimi asubuhi kwa asubuhi; huyaamsha masikio yangu kama
wale wanofundisha. 5 Bwana Yahwe amefungua sikio langu, na sikuaasi, wala kurudi
nyuma. 6 Niliwapa mgongo wangu wale wanaonipiga mimi, na shavu langu kwa
wale wanaopokonya nje ndevu zangu; Sitouficha uso wangu kutokana na matendo
ya aibu na kutema mate. 7 Maana Bwana Yahwe atanisaidia mimi; hivyo basi
sitapatwa na aibu; hivyo nimeufanya uso wangu kama jiwe, maana ninajua kwamba
sitaabishwa. 8 Yeye aliye nitakasa mimi yu karibu. Ni nani atakayenipinga mimi?
Basi na tusimame tufarijiane mmoja mmoja. Nani aliye mshitaki? Muache aje karibu

na mimi. 9 Tazama, Bwana Yahwe atanisaidia mimi. Nani atakayetangaza kuwa
mimi ni mwenye hatia? Tazama, watavaa nje kama vazi; mdomo utawala wao juu.
10 Ni nani miongoni mwenu anayemuogopa Yahwe? Ni nani anayehieshimu sauti ya
Yahwe? Ni nani atakayetembea kwenye giza nene pasipo mwanga? 11 Tazama, ninyi
nyote mnaowasha, ni nani aliyewapa wenyewe kwa tochi: tembeni katika mwanga
wa moto wenu na katika moto mliouwasha. Hili ndilo mlilopokea kutoka kwangu:
utalala chini katika mahali pachungu.

# 51

1 Nisikilizeni mimi, enyi mtendao haki, enyi mtafutaye Yahwe: Tazama katika
mwamba uliouchonga nakuchimba kutoka pale ulipopakata. 2 Mtazameni Ibrahimu,
baba yenu, na Sara, aliyewazaa ninyi; maan alipokuwa na upweke yeye mwenyewe,
Nilimuita yeye. Nikambariki yeye na kumfanya yeye kuwa wengi. 3 Ndio, Yahwe
ataifariji Sayuni; Ataifariji miji yake yote iliyo na ukiwa; jangwa lake atalifanya
kama Edeni, na jangwa lililo wazi pembeni ya bonde la mto Yordani kama bustani
ya Yahwe; Furaha na shangwe vitakuwa kwake, shukrani, na sauti ya kuimba.
4 "Kuwa makini kwangu, watu wangu; na nisikilizeni mimi, watu wangu! Maana
nitatoa amri, na nitaifanya haki yangu kuwa sheria ya mataifa. 5 Haki yangu ipo
karibu; wokovu wangu utaenda nje, na mikono yangu itahihukumu mataifa; Pwani
itanisubiri mimi; maana wanashauku ya kuhusubiria mkono wangu. 6 Nyanyueni
macho yanu juu angani, na tazama nchi chini, maana mbingu zitatoweka mbali
kama moshi, na nchi itachakaa kama vazi, na wenyeji wake watakufa kama inzi.
Lakini wokovu wangu utaendelea daima, na haki yangu haitaacha kutenda kazi.
7 Nisikizeni mimi, enyi mnaotambua ukweli, enyi watu wangu mliobeba sheria
yangu katika mioyo yenu: Msiogope matusi ya watu, wala kukatishwa tamaa na
unyanyasaji wao. 8 Maana Nonda watawala wao kama vazi, na minyoo itawala
wao kama sufu; lakini haki yangu itakwa daima, na wokovu wangu katika vizazi
vyote." 9 Amka, amka, jivishe wewe mwenyewe kwa nguvu, mkono wa Yahwe.
Amka kama siku za zamani, kizazi cha nyaktii za kale, Je sio wewe uliyeangamiza
mnyama wa baharini, na uliyemchoma joka? 10 Je haukukausha bahari, maji ya
kina kirefu, na kufanya kina cha bahari kuwa nija ya ukombozi kupita? 11 Fidia ya
Yahwe itarudi na kwenda Sayuni kwa kilio cha furaha na furaha ya milele itakuwa
katika vichwa vyao, na huzuni na kuomboleza vitatoweka mbali. 12 "Mimi, mimi
ndiye niwapae faraja. Kwa nini uwaogope watu, ambao wanakufa, watatoto wa
wanadamu, waliofanywa kama majani? 13 Kwa nini umemsahau Yahwe Muumba,
yeye azinyooshayembingu na kuweka misingi ya nchi? Nyie ambao mna hofu za
mara kwa mara kila siku kwa sababu ya hasira ya moto ya wanyanyasaji anapo
fanya maamuzi ya kuangamiza. Iko wapi hasira ya wanyanyasaji? 14 Yeye aliyeinama
chini, Yahwe atafanya haraka kumuachia; hatakufa wala kwenda chini katika shimo,
wala hatakosa mkate. 15 Maana Yahwe Mungu wenu, anaye ifanya bahari itembee,
hivyo mawimbi yake yavume kwa kishindo- Yahwe wa majeshi ndilo jina lake.
16 Niweka maneno yangu mdomoni mwako, na nimekufunika wewe kwa kivuli cha
mkono wangu, ili niweze kupanda mbingu, kuweka misingi ya nchi, na kutamkia
Sayuni, 'ninyi ni watu wangu." 17 Amka, amka, simama juu, Yerusalemu, ewe
unyweae katika kikombe cha hasira ya Yahwe kutoka mkononi mwako; umekunjwa
katika kikombe, kikombe cha mateso, na umekunjwa na kumaliza. 18 Hakuna hata
mmoja miongoni mwa watoto aliyewazaa wa kumuongoza yeye; hakuna hata mmoja
miongoni mwa wote aliyewalea wa kumshika mkono wake. 19 Shida hizi mbili
ziliwatokea ninyi- ni nani atahuzunika pamja nanyi? - ukiwa na uharibifu, na njaa
na upanga. Ni nani atakayekufariji wewe? 20 Watoto wako walizimia; walilala kila

kona ya mtaa, kama swala kwenye mtego; Wamejawa na hasira ya Yahwe, Laana ya
Mungu wako. 21 Lakini sasa sikiliza hili, ewe uliodhulumiwa na kulewa, lakini sio
kwa mvinyo: 22 Bwana wenu Yahwe Mungu, anayewasihi watu wake, asema hivi,
''Tazama, Nimechukua kikombe cha ukubwa mkononi mwako- ukubwa wa kikombe
cha hasira yangu - ili usiweze kunjwa tena. 23 Nitakuweka kwenye mikono ya
watesaji, wale waliokuambia wewe, Lala chini, ili tutembee juu yako'; wameufanya
mgongo wako kama uwanjwa na kama wao wa.''

# 52

1 Amka, amka, vaa nguvu zako, Sayuni; vaa vazi lako zuri, mji mtakatifu; maana
hakuna tena kutotahiriwa wala wasio safi kuingia kwako. 2 Jikung'ute mwenyewe
kutoka mavumbini; nyanyuka na ukae, ewe Yerusalemu; ondoa shanga katika shingo
yako, wafungwa, binti ya Sayuni. 3 Maana Yahwe asema hivi, umeuzwa bure, na
utakombolewa pasipo pesa.'' 4 Maana Bwana Yahwe asema hivi, ''Hapo mwanzo watu
wangu walishuka chini Misri kuishi kwa muda mfupi; Waasiria waliwanyanyasa wao
hivi karibuni. 5 Sasa ni kitu gani nilicho nacho hapa- Hili ni tamko Yahwe- aonae
kwamba watu wake wanachukuliwa bure tu? Wale wanowaongoza wao wanafanya
mzaha-Hili ni tamko la Yahwe- jina langu linakashifiwa mchan kutwa. 6 Hivyo basi
watu wangu watalijua jina langu; watajua kwamba siku hiyo kwamba mimi ndiye
ninayesema ''Ndiyo, Ni Mimi!'' 7 Ni kwa uzuri gani juu miliima ni miguu ya mjumbe
aliyeleta habari njema, atangazae amani, aliyebeba uzuri wa ukuu, aliyetangaza
wokovu, anayesema kwa Sayuni, ''Mungu wako anatawala!'' 8 Sikiliza enyi walinzi
nyanyueni sauti zenu, kwa pamoja pigeni kelele kwa furaha, maana mtamuona, kwa
kila jicho lenu, kurejea kwa Yahwe Sayuni. 9 Pazeni sauti kwa kuimba kwa furaha,
enyi mateka wa Yerusalemu; maana Yahwe amefariji watu wake; ameikomboa
Yerusalemu. 10 Yahwe amewaonyesha kwamba mkono wake mtakatifu katika macho
ya mataifa yote; nchi yote itauona wokovu wa Mungu wetu. 11 Ondokeni, ondokeni,
enendeni mbali na hapa; msiguse kitu chochote ambacho ni najisi; au kuishi katikati
yake; jitakase mwenyewe, enyi mliobeba vyombo vya Yahwe. 12 Maana hautakwenda
nje kwa kukimbia, wala hautaondoka kwa hofu; Maana Yahwe atakuwa mbele yako;
na Mungu wa Israeli atakuwa mlinzi wako nyuma. 13 Tazameni, mtumishi wangu
atafanya hekima; atakuwa juu na atanyanyuliwa juu, na atapandishwa juu. 14 Na
wengi watamstajabia yeye- muonekano wake umekunjamana nje ya muonekano wa
mwanadamu, hivyo basi upande wake ulikuwa mbali na kitu chochote ambacho
ni binadamu- 15 Na hivyo, mtumishi wangu atanyunyizia mataifa mengi na wafme
watafunga midomo yao kwa sababu yake. Kana kwamba hawajawahi kuambiwa,
wataona, kana kwamba hawakusikia, wataelewa.

# 53

1 Ni nani angeweza kuamini tuliyasikia? Na mkono wa Yahwe, kwake uliojidhi-
hirisha? 2 Maana amekuwa mbele za Yahwe kama sampuli, na kama chipukizikatika
aridhi kavu; hakuna maajabu yalionekana au mapambo; tulipo muona yeye,
hapakuwa na uzuri kutuvutia sisi. 3 Alidharauliwa na kukataliwa na watu; mtu wa
huzuni, na mwenye maumivu. Kama mmoja aliyetoka kwa watu wafichao nyuso
zao, alidharauliwa; na kujfikiria kuwa asiye na faida. 4 Lakini hakika amezaliwa
ugonjwa wetu na kubeba huzuni yetu; tulidhani aliadhibiwa na Mungu, amepigwa
na Mungu, na kutaabishwa. 5 Lakini alichomwa kwa sababu ya uaasi wa matendo
yetu; aliangamizwa kwa sababu ya dhambi zetu. Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu
yake, na kwa majeraha yake sisi tumepona. 6 Sisi ni kama kondoo tumepotoka; kila
mmoja amejeuka katika njia yake, na Yahwe amemueka juu yake maovu kwetu sisi

sote. 7 Aliteswa; lakini alinyenyekea mwenyewe, hakufungua mdomo wake; kama
kondooendae kuchinjwa, na kama kondoo mbele ya mtu anayemkata mnyoa yake
taratibu, hivyo hakufungua mdomo wake. 8 Kwa kutumia nguvu na hukumu yeye
aliyelaaniwa; ni katika kizazi hicho atafikiria zaidi kuhusu yeye? Lakini aliondolewa
katika aridhi ya walio hai; kwa sababu ya makosa ya watu wangu na adhabu
ilikuwa juu yake. 9 Wameliweka kaburi lake pamoja nawahalifu, kwa utajiri wa
mtu katika kifo chake ingawa hakuwa na vurugu wala udanganyifu wowote katika
mdomo wake. 10 Lakini yalikuwa ni mapenzi ya Yahwe kumponda yeye na kumfanya
yeye apone. Alipoyafanya maisha yake kuwa sadaka kwa ajili ya dhambi, ataona
watoto wake, ataongeza siku zao, na mapenzi ya Yahwe yatatimizwa kupitia yeye.
11 Baada ya mateso ya maisha yake, ataona mwanga na ataridhika kwa maarifa yake.
12 Hivyo basi Je ninaweza kumpa yeye sehemu yake miongoni mwa wengi, naye
atatawnya mateka kwa wengi, kwa sabubu amejionyesha yeye mwenye kwenye kifo
na amehesabiwa na wahalifu. Amezaa dhambi za wengi na kufanya maombolezo
kwa wahalifu.

# 54

1 "Imba, ewe mwanamke tasa, ewe ambaye haujazaa; imba wimbo kwa furaha na
lia kwa nguvu ewe ambaye hujapata uchungu wa kuzaa. Maana watoto walio katika
ukiwa ni wengi kuliko watoto wa wanawake waliolewa," asema Yahwe. 2 Fanya hema
lako kuwa kubwa na tawanya mapazia mbali, sio kidogo; nyoosha kamba zako na
imarisha vigingi vyako. 3 Maana utawanjwa katika mkono wa kulia na wa kushoto,
na ukoo wako utashinda mataifa na kuwapatia miji iliyo na ukiwa. 4 Usiogope maana
hautahaibika, wala kukatishwa tamaa maana hautapatwa na aibu; hutasahau aibu
ya ujana wako na aibu ya kutelekezwa. 5 Maana Muumba ni mume wako; Yahwe wa
majeshi ndilo jina lake. Mtakatifu wa Israeli yeye ni mkombozi wenu; anaitwa Mungu
wa nchi yote. 6 Yahwe anakuita wew urudi kama mwanamke aliyetelekezwa na
mwenye roho ya huzuni, kama mwanamke mdogo aliyeolewa na kukataliwa, asema
Mungu. 7 "Kwa kipindi kifupi nimewatelekeza ninyi, lakini kwa huruma kubwa
nitawakusanya ninyi. 8 Katika gharikia ya hasira nimeuficha uso wangu kwa muda.
lakini kwa agano la milele la kuaminika nitakuwa na huruma na ninyi- amesema
Yahwe, aliyewakomboa ninyi. 9 Maana haya ni kama Nuhu kwangu: kama nilivyoapa
maji ya Nuhu hayuatapita tena katika nchi, Hivyo nimeapa kwama sitapatwa na
hasira na ninyi wala kuwakemea ninji. 10 Japo milima yaweza kuanguka na vilima
vyaweza kutikiswa, japo uimara wa pendo langu hautageuka nyuma kutoka kwenu,
wala agano langu la amani kutikiswa- asema Yahwe, Yeye mwenye huruma juu yenu.
11 Wanaotaabika, wanaopitia dhoruba na wasio na faraja, tazama, nitaweka lami kwa
rangi nzuri, na kuweka misingi kwa yakuti. 12 Nitaufanya mnara wa akiki na lango
yake ya almasi na kuta zake za nje ni za mawe mazuri. 13 Na watoto wako wote
watafundishwa na Yahwe; na amani ya watoto wako itakuwakubwa. 14 Katika haki
nitakuanzisha tena. Hautaona dhiki tena, maana hautaogopa, na hakuna kitu cha
kutisha kitakachokuja karibu yako. 15 Tazama, ikiwa yeyote atakaye koroga matatizo,
hayatako kwangu; yeyote atakaye changanya matatizo pamaoja na wewe ataanguka
kwa kishindo. 16 Tazama, nimemumba fundi, anayepuliza makaa yanayoungua na na
kuanda a silsha kama kazi yake, na nimemumba mharibifu ili awaharibu. 17 Hakuna
silaha iliyotengenezwa dhidi yako ikafanikiwa; na utamlaani kila mmjoa anayekutusi
wewe. Huu ndio urithi wa watumishi wa Yahwe, na uthibitisho wake kutoka kwangu-
Hili ndilo tamko la Yahwe."

# 55

1 "Njooni, kila aliye na kiu, njooni kwenye maji! na ewe usio na pesa, njoo, ununua

na ule! Njoo, nunua mvinyo na maziwa pasipo pesa na pasipo gharama. 2 Kwa
nini tunapima fedha kwa kitu ambacho sio mkate? na kufanya kazi isiyoridhisha?
Nisikilizeni mimi kwa makini na ule kilicho kizuri, na kujifurahisha mwenyewe kwa
unono. 3 Jeuzeni masikio yenu, na mje kwangu! Sikiliza, iliuweze kuishi! Nitafanya
agano ya milele na ninyi; pendo langu la kuaminika nililomuhaidi Daudi. 4 Tazama,
nimwemuweka yeye kama shahidi kwa mataifa, kama kiiongozi na kamanda wa
watu. 5 Tazama, utaliita taifa ambalo haulijui; na taifa ambalo halikujui wewe
litakukimbilia wewe kwa sababu wewe ni Yahwe Mungu wao, Mtakatifu wa Israeli,
yeye aliyekutukuza wewe. 6 Mtafuteni Yahwe maana anapatikana; muiteni yeye
maana yu karibu. 7 Tuwaache waovu waziache njia zao, na mtu mwenye dhambi
mawazo yake. Muache yeye arudi kwa Yahwe, na atamuhurumia yeye, na kwa
Mungu wetu, yeye ambaye atamsamehe huyo kwa wingi. 8 Maana mawazo yangu
sio mawazo yenu, wala njia zangu sio njia zenu- Hili ni tamko la Yahwe- 9 maana
kama vile mbingu zilivyo juu kuliko nchi, hivyo ndivyo njia zangu zilivyo juu kuliko
njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu. 10 Maana kama mvua na theluji
zishukavyo chini kutoka mbinguni na hazirudi tena pale isipokuwa kueneza nchi
na kufanya uzalishaji na chipukizi na kutoa mbegu kwa wakulima waliopanda na
mkate kwa walaji, 11 hivyo neno langu litakuwa linalotoka kwenye mdomo wangu:
halitanirudia tena mimi bure, Lakini itatimiza lilie nililokusudia, na litatimiza lile
nililolituma. 12 Maana utakwenda nje katika furaha na utaongozwa kwa amani;
Milima na vilima vitapaza sauti kwa furaha mbele yako, na miti yote shambani
itapiga makofi. 13 Badala ya miiba ya porini, misonobari itakuwa; na badala ya
mbigiri, mihadasi inaota, na itakuwa kwa Yahwe, maana jina lake, ni kama alama ya
milele ambayo haiwezi kuondolewa."

# 56

1 Yahwe asema hivi, "Fanyeni yaliyo sahihi, fanyeni yaliyo ya haki; maana wakovu
wangu u karibu, na haki yangu inakaribia kujidhihirisha. 2 Abarikiwe mtu yule
ataendae haya, anayeyashika sana. Anaifuata sabato, na haitii unajisi, azuiaye mkono
wake usitende maovu." 3 Usimuache mgeni yeyote aliyekuwa mfuasi wa Yahwe
aseme, "Yahwe atahakikisha ananiondoa kwa watu wake." Toashi ataweza kusema,
"tazama, mimi ni mti mkavu." 4 Yahwe asema hivi, kwa matoashi wanaoitimiza
sabato yangu huchagua mambo yanayonipendeza mimi, na hushika kwanza agano
langu, 5 kwao nitaiweka nyumba yangu na ndani ya kuta zangu kumbukumbu
ambayo ni kubwa kuliko kuwa na vijana na mabinti. Nitawapa kumbumbu ya milele
ambalo halitaondolewa. 6 Pia wageni ambao wataungana wenyewe kwa Yahwe- kwa
ajili ya kumtumikia yeye, na yeye alipendae jina la Yahwe, kumuabudu yeye, na
kila anayeheshimu sabato na wale wanoitunza isitiwe najisi, na wale walishikao
agano langu 7 nitawaleta katika mlima wangu mtakatifu na kuwafaya muwe na
furaha katika nyumba yangu ya maombi; matoleo na sadaka zenu zitakubalika katika
mathebau yangu. Maana nyumba yangu itaitwa nyumba ya maombi kwa mataifa
yote. 8 Hili ni tamko la Yahwe, anayewakusanya watu wenye ukiwa katika Israeli-
nitaendelea kuwakusanya wenginwe ili kuwaongeza wao." 9 Enyi nyote wanyama
pori mlioko porini, njooni na mle, enyi wanyama mlioko msituni, Walinzi wao wote ni
vipofu, hawaelewi. 10 Wote ni mbwa wapole ambao hawawezi kubweka. Wanaota, na
wanalala chini maana wanapenda kulala. 11 Mbwa wanahamu kubwa; hawajawahi
kuridhika; wachungaji wao hawawatambui; wamejeuka katika njia zao wenyewe,
kila mmoja ana tamaa kupata faida isiyo yaa haki. 12 "Njooni, "Tunywe mvinyo na
pombe. Kesho itakuwa kama leo, siku kubwa zaidi ya kipimo."

# 57

[1] Wenye waki watatoweka, lakini hakuna mtu atakayelitia maanani, na watu
wa agano la kuaminika wamekusanyika mbali, lakini hakuna mtu anayefahamu
kuwa wenye haki wamekusanyika mbali na maovu,. [2] Wameingia katika amani;
wamepumzika katika vitanda vyao, wale wanotembea katika haki. [3] Lakini njooni
hapa, enyi watoto wa wachawi, watoto wa wazinifu na mwanamke anayefanya
ukahaba. [4] Ni nani mnayemfanyia mzaha? dhidi ya wale wanofungua midomo
yao na kutoa nje ndimi zao? Je ninyi sio watoto wa uaasi, watoto wa uongo?
[5] Enyi unaowasha wenywe kwa kulala pamoja chini ya mualoni, kila chini ya mti
mbichi, ewe unaeua watoto wako katika mabonde yaliyokauka, chini ya miamba
inayoning'inia. [6] Miongoni mwa vitu vilaini katika bonde la mto ni mambo uliyopewa
uyafanyie kazi. Ni vitu vya ibada yako. Umemwaga nje kinywaji chako kwao na kutoa
sadaka ya mazao. Katika haya mambo Je ninaweza kuwa radhi na mambo haya?
[7] Umeandaa kitanda chako juu ya mlima mrefu; pia umeeda pale juu kutoa sadaka.
[8] Nyuma ya mlango na mihimili ya milango umeweka ishara zako; umeniweka mimi
furagha, umejifunua wewe mwenywe, na kwenda juu; umekifanya kitanda changu
kuwa kikubwa. Umefanya agano na wao; ulipenda vitanda vyao; uliona sehemu zao
za siri. [9] Ulienda kwa Moleki pamoja na mafuta; umeongeza marashi. Ulimtuma
balozi wako mbali sana; Alikwenda chini kuzimu. [10] Ulichoka kwa safari yako
ndefu, lakini haukusema, ''Haina matumaini.'' Umeyatafuta maisha katika mkono
wako; Hivyo basi haukudhoofika. [11] Ni uliyemuogopa? Ni nani uliye muhofia
zaidi ambaye aliyekufanya wewe kutenda udanganyifu, kwa wingi namna hiyo
ambapo hauwezi kunikumbuka mimi au kufikiria kuhusu mimi? Maana nilikuwa
kimya kwa mda mrefu, hauniogopi mimi tena. [12] Nitatangaza matendo haki yako
na nitawaambia kila kitu ulichokifanya, lakini hawatakusaidia. [13] Utakapolia nje,
wacha sanamu ulizozikusnya zikusaidie wewe. Badala yake upepo utavipeperusha
vyote, punzi itavipeperusha mbali. Lakini yeye anayenikimbilia mimi atairithi
aridhi na atachukua umiliki katika mlima wangu mtakatifu. [14] Atasema, 'Jenga,
jenga! safisha njia! ondoeni vizuizi vyote katika njia ya watu wangu!'' [15] Maana
yeye allye juu palipoinuka, anayeishi katika uzima wa milele, ambaye jina lake ni
mtakatifu, asema hivi, ''Ninaishi mahali pa juu na mahali patakatifu pamoja na yeye
pia aliyemnyenyekevu na moyo uliopondeka, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu
na kufufua mioyo ya wanaojutia. [16] Maana sitawahukumu milele, wala sitakuwa
na hasira milele, Kisha roho ya mtu itazimia mbele yangu, maisha niliyowafanyia.
[17] Kwa sababu ya dhambi ya mapato ya vurugu zake, Nilipatwa na hasira, na
nikamuadhibu yeye; niliuficha uso wangu, nilikuwa na hasira, lakini alirudi nyuma
katika njia za moyo wake mwenyewe. [18] Nimeziona njia zake, lakini nitamoponya
yeye. Nitamuongoza yeye na kumfariji na kuwashauri wale wanomliliia yeye, [19] na
natengeneza tunda la midomo. Amani, amani, kwa wale walio mbali sana na wale
walio karibu-asema Yahwe nitawaponya ninyi. [20] Lakini waovu ni kama bahari
iliyochafuka, haiwezi kutulia, na maji yake yametanda juu ya matope. [21] Hakuna
amani kwa wakosaji asema Mungu.''

# 58

[1] ''Lia kwa sauti; usinyamaze. Paza sauti yako juu kama mbiu. Kabiliana na
watu wangu wenye uasi, na nyumba ya Yakobo na dhambi zao. [2] Bali wananitafuta
mimi kila siku na kufurahia katika maarifa ya njia zangu, kama taifa linalotenda
haki na hawakuiacha sheria ya Mungu wao. Wananiuliza mimi kuhusu hukumu ya
haki; wamepata furaha katika mawazo yao ya kwa kumkaribia Mungu [3] Kwa niini
tulifunga; walisema, 'Lakini hamkuona hilo? Kwa nini tulijinyenyekeza wenywe,

lakini hakutambua?' Tazama, siku ya kufunda kwanu utatafuta furaha yanu
mwenyewe na kuwanyanyasa wafanyakazi wenu wote. 4 Tazama, ninyi mnafunga
ili muwe wepesi wa kugombana na kupigana, na kupiga kwa ngumi ya uovu wako;
haujafunga leo kuifanya sauti yako isikike juu. 5 Kwa uhalisi aina ya mfungo huu
ndio ambao ninauhitaji: Siku ambayo kila mtu hunyenyekea mwenyewe, huinamisha
kichwa chake chini kama mwanzi, na hutawanya mavazi ya magunia na majivu chini
yake? Je kweli unauita huu ni mfungo, siku ya kumfurahisha Yahwe.? 6 Hii sio
mfungo ambao niliuchagua mimi: kufungua vifungo vya waovu, kufungua kamba
za nira, kuwaweka huru walioangamizwa, na kuharibu kila nira? 7 Sio kwamba
kula mkate na wenye njaa na kuwaleta masikini na kuwaleta wasio na makazi
katika nyuma yako?" Unapomuana mtu yuko uchi, unatakiwa vumvishe mavazi;
na usijifiche mwenyewe na ndugu zako. 8 Halafu mwanga wako utafunguliwa kama
jua, na uponyaji wako utachipukia juu kwa haraka; haki yako itaenda mbele zake,
na na utukufu wa Yahwe utakuwa nyuma kukulinda. 9 Halafu utamuita, na Yahwe
atakuitikia; utalia ukihitaji msaada, na atasema, "Nipo hapa." Ikiwa utaitoa nira
isiwepo miongoni mwako, kidole kinachoshataki, maongezi ya waovu, 10 Ikiwa wewe
mwenyewe utawapa wenye njaa na kuwaridhisha wahitaji katika shida, na giza
lako litakuwa kama mchana. 11 Halafu Yahwe ataendelea kuwaongoza ninyi na
kuwa ridhisha ninyi katika mikoa ambayo hakuna maji, Ataimarisha mifupa yenu.
Mtakuwa kama bustani iliyonyeshewa maji, na kama mkondo wa maji, ambaopo
maji yake hayapungui. 12 Baadhi yenu mtajenga tena sehumu za kale zilizoharibiwa;
mtatengeneza sehemu zilizoharibiwana vizazi vingi; na mtaitwa "Mrekebishaji wa
ukuta," kuwarejesha katika mtaa ya kuishi." 13 Tuseme kwamba ukigeuza nyuma
miguu yenu kutoka safarini katika siku ya sabato, kufanya anasa siku yangu takatifu,
Tuseme kwamba umeiita sabato siku ya furaha, na umeiita siku ya Bwana Yahwe
mtakatifu na yenye kuheshimiwa. Tuseme kwamba unahieshimu sabato kwa kuacha
biashara zako, na hautafuti anasa zako mwenyewe na uzungumzi maneno yako
mwenyewe. 14 "Halafu utapata furaha kwa Yahwe; na nitaifanya safari yako juu
ya urefu wa nchi; Nitakulisha wewe kwenye urithi wa Yakobo baba yenu- maana
mdomo wa Yahwe umezungumza."

# 59

1 Tazama, mkono wa Yahwe sio mfupi ambao hautweza kukuokoa wewe; wala
sikio lake sio zito, ambalo haliwezi kusikia. 2 Matendo yako ya dhambi, hata
hivyo, zimekutenga wewe na Mungu, na dhambi zenu zimemfanya aufiche uso
wake msimuone wala kumsikia yeye. 3 Maana mikono yenu ina madoa ya damu
na vidole vyenu vimejaa dhambi. Midomo yenu inazungumza uongo na ulimi
wenu unazungumza kwa nia mbaya. 4 Hakuna hata mmoja aitae haki, na hakuna
anayewasihi kesi yake katika haki. Wanayamini maneno yasiyo ya haki, maneno ya
uongo; wanashika matatizo na kuzaa dhambi. 5 Wanetotoa mayai ya nyoka wenye
sumu na hufuma mtandao wa buibui. Yeyote alaye mayai yake atakufa, na ikiwa
yai litavunjika, litatotoa nyoka mwenye sumu. 6 Mitando yao haitatumika kama
mavazi, wala hawawezi kujifukia wenyewe kwa kazi yao. Kazi zao ni kazi za dhambi,
na matendo ya vurugu yako mikononi mwao. 7 Miguu yao inakimbilia uovu, na
wanakimbilia kumwaga damu isiyo na hatia. Mawazo yao ni mawazo ya dhambi;
vurugu na uharibifu ndio njia yao. 8 Njia ya amani hawaijuyui, na hakuna haki katika
njia zao. Wametengeneza njia njia zlizopotoka; yeyote atakaye safiri kupitia njia hizi
njia hizi hazijui amani. 9 Hivyo basi haki iko mbali a sisi, wala haki haijatufikia
sisi. Tunasubiri mwanga tunaona giza; tunatafuta mwangaza, lakini tunatembea
gizani. Tunapapasa kwenywe ukuta kama kipofu, kama wale wasiona, 10 Tuna

mashaka mchana kweupe kama kwenye mwanga unaofifia; miongoni mwa wenye
nguvu tuko kama watu waliokufa. 11 Sisi tunaunguruma kama dubu na kuomboleza
kama njiwa; tunasubiria haki, lakini hakuna kitu; kwa ukombozi, lakini uko mbali na
sisi. 12 Maana makosa yetu mengi yako mbele zako, na dhambi zetu zinatushuhudia
sisi; maana makosa yako pamoja na sisi. 13 Tumeaasi, kumkana Yahwe na kuacha
kumfuata Mungu. Tulizungumzia ulafi kujeuka nyuma, na kuanza kulalamika kutoka
moyoni na maneno ya uongo. 14 Haki imerudishwa nyuma, wenye haki wamesimama
mbali sana; maana ukweli uko mashakani katika mraba wa umma, haki haiwezi
kuja. 15 Waaminifu wamenda zao, na yeyote anayegeuka mbali na maovu anajiathiri
mwenyewe. Yahwe aliliona hilo na hakupendezwa maana hakuna haki. 16 Aliona
kwamba hakuna mtu, na akastaajabu kwamba hakuna mtu wa kuoma. Hivyo basi
mkono wake ulileta wakovu kwake, na haki yake unamtosheleza yeye. 17 Huivaa
haki kama ngao kifuani na kofia ya chuma ya wokovu kichwani mwake. Anajivika
mwenyewe kwa mavazi ya kisasi na kuvaa vazi la bidii. 18 Analipa tena kwa
kilichotokea, hukumu ya hasira kwa adui zake na kwa adui atairidisha adhabu ya
kisiwa kama zawadi yao. 19 Hivyo wataliogopa jina la Yahwe kutoka magharibi na
utukufu wake kutoka mashariki; maana atakuja kama mkondo wa mto, inaendeshwa
na pumzi ya Yahwe. 20 Mkombozi atakuja Sayuni na wale watkaojeuka kutoka
matendo yao ya uasi katika nyumba ya Yakobo- Hili ni tamko la Yahwe. 21 Na kama
mimi, hili ni agano langu pamoja nao- asema Yahwe- Roho yangu iliyo juu yenu, na
maneno yangu niliyoyaweka kinywani mwenu, hayataondoka midomo mwenu au
kuodoka mbali na midomo wajukuu wenu, au kwenda mbali asema Yahwe- kuanziia
sasa na hata milele.''

# 60

1 Nyanyuka, uangaze; maana mwanga wako umekuja, na utukufu wa Yahwe
umekuja kwako. 2 Japokuwa giza litatanda katika nchi, na giza nene katika mataifa;
Lakini Yahwe atakuja juu yenu, na utukufu wake utaonekana kwenu. 3 Mataifa
yatakuja kwenye mwanga wako, na wafalme katika mwanga wako mkali uliokuja
4 Tazama na angalia pande zote. Wamekusanyika wao wenyewe kwa pamoja na
wanakuja kwako. Watoto wako watatoka mbali, na binti zao watabebwa katika
mikono yenu. 5 Halafu wataangalia na kuwa furaha, na moyo wako utafurahia na
kufurika, maana wingi wa maji utamwagwa juu yenu, utajiri wa mataifa utakuja
kwenu. 6 Msafara wa ngamia utawafunika ninyi, na ngamia wa Midiani na Efa;
wote watakuja kutoka Sheba; wataleta dhahabu na ubani, wataimba sifa kwa Yahwe.
7 Makundi yote ya Kedari yatakusanika kwa pamoja kwako, kondoo wa Nebaioti
watabeba mahitaji yako; watakubalika kutolewa sadaka katika madhebau yangu;
na nitaitukuza nyumba yangu takatifu. 8 Ni nani hawa wanopaa wenyewe kama
mawingu, na kama njiwa kwenye makazi yao? 9 Pwani itanitafuta mimi, na meli ya
Tarshishi huwaongoza, huwaleta watoto wenu kutoka mbali, pamoja na fedha zao
na dhahabu zao, maana jina la Yahwe Mungu wenu, na Mtakatifu wa Israeli, maana
amekuheshimu wewe. 10 Watoto wa wageni watajenga tena kuta zenu, n awafalme
wao watawatumikia ninyi; japo katika laana yangu nimewaadhibu ninyi, lakini
kwa neema yangu nitawahurumia ninyi. 11 Milango yenu itaendelea kuwa wazi;
haitafungwa mchana au usiku, hivyo utajiri wa mataifa ili uweze kuletwa, pamoja na
viongozi wanowaongoza. 12 Kweli, mataifa na falme ambayo hayatakutumikia wewe
yatatoweka; mataifa hayo yataangamizwa kabisa. 13 Utukufu wa Lebanoni utakuja
kwako, mti wa msonobari, mtidhari, pamoja na msonobari ili kupamba madhebau
yangu; na Nitalitukuza eneo la miguu yangu. 14 Watakuja kwako kukusujudia wewe,
watoto wa wale wanaokunyenyekea wewe; wataisujudia miguu yako; watakuita

wewe mji wa Yahwe, sayani ya Mtakatifu wa Israeli. [15] Badala yake uwepo wenu
umetelekezwa na kuchukiwa, kwa kuwa hakuna hata mmoja anayepita ndani yenu,
nitawafanya kuwa kitu cha kiburi milele, furaha kutoka kizazi hata kizazi. [16] Pia
utakunywa maziwa ya mataifa, utatunzwa katika kifua cha wafalme; utajua kwamba
Mimi Yahwe, Mimi ni mwokozi na mkombozi wenu, aliye Mkuu wa Israeli. [17] Badala
ya shaba Nitaleta dhahabu, badaia ya chuma nitaleta fedha; badala ya mbao, shabana
badala ya jiwe, chuma. Nitachagua amani kwa kiongozi wenu, na haki kiongozi
wenu. [18] Vurugu hazitasikika katika aridhi yenu, uharibifu wala uvunjaji katika
mipaka yenu; lakini mtaita kuta zenu wokovu, na malngo yenu mtayaita sifa. [19] Jua
halitakuwa mwanga wenu wakati wa mchana, wala mwanga wa mwenzi wakati
wa usiku hautawawakia ninyi; Lakini Yahwe atakuwa mwanga wenu wa milele, na
Mungu wenu na utukufu wenu. [20] Jua lenu halitakuewepo wala mweni utaondoshwa
na kutoweka; maana Yahwe atakuwa mwanga wenu daima, na siku za maombolezo
zitakwisha. [21] Watu wako wote watakuwa wenye haki; watachukuwa urithi wa nchi
kwa mda wote, tawi la mazao yangu, kazi ya mikono yangu, ili niweze kuitukuza.
[22] Mtoto atakuwa maelfu, na mdogo atakuwa taifa la wenye nguvu; Mimi Yahwe
Nitayatimiza hayo mda utakapowadia.

# 61

[1] Roho ya Bwana Yahwe i juu yangu, maana Yahwe amenipaka mafuta mimi
kuhiubiri habari njema kwa wenye taabu. Amenituma mimi kuwaponywa waliopon-
deka mioyo, kutangaza uhuru kwa wafungwa, na kufungua gereza ili waliofungwa
waweze kutoka. [2] Amenituma mimi kuutangaza mwaka wa Yahwe uliokubalika, siku
ya kisasi cha Mungu wetu, na kuwafariji wale wote wanaomboleza. [3] Amenituma
mimi - kuwapa wale waoombolezao katika Sayuni -kuwapa wao kilemba cha majivu,
mafuta ya furaha badala ya kuomboleza, vazi la kusifu katika eneo la roho ya ubutu,
kuwaita mialoni ya haki, iliyooteshwa na Yahwe, ili aweze kutukuzwa. [4] Wataijenga
tena mahali pa kale palipohaibiwa; wataparejesha mahali palipokuwa na ukiwa.
Watairejesha miji iliyoharibiwa, Mahali penye ukiwa kutoka vizazi vingi vilivyopita.
[5] Wageni watasimama na kulisha makumdi yako, na watoto wa wageni watafanya
kazi kwenye mashamba yako na mizabu. [6] Mtaitwa makuhani wa Yahwe; watawaita
watumishi wa Mungu wetu. Mtakula utajiri wa mataifa, na utajivuinia katika utajiri
wake. [7] Badala yake aibu yenu itaongezeka; na badala ya fedhea walifurahia juu
ya sehemu yao. Hivyo basi sehemu yao itaongezeka mara mbili katika nchi na
furaha ya milele itakuwa yao. [8] Maana Mimi, Yahwe, ninapenda haki, na ninachukia
wizi na vurugu zisizo za haki. Nitawalipa wao kataka haki na Nitafanya agano
la milele na wao. [9] Uzao wao utajulikana miongoni mwa mataifa, na watoto wao
miongoni mwa watu. Wote watakaowaona watawakubali wao, kwamba ni watu
wangu ambao Yahwe amewabariki. [10] Nitafurahia sana katika Yahwe; Katika Mungu
nitafurahia. Maana amenivika mimi kwa vazi la wokovu; amenivika mimi kwa vazi
la haki, kama bwana harusi aliyejipamba mwenywe kwa kilemba, na kama bibi
harusi aliyejipamba kwa vito. [11] Maana kama nchi inavyozalisha miti inayochipukia
na kama bustani inavyofanya miti yake ikuie, hivyo Bwana atasasbabisha haki na
sifa kuchipukia mbele ya mataifa yote.

# 62

[1] Kwa niaba ya Sayuni sitatulia, na kwa naiba ya Yerusalemu sitanyamaza kimya,
mpaka haki yake itakapotokea, na wokovu wake kama tochi. [2] Mataifa yataona haki
yako, na wafalme wote wataona utukufu wako. Utaitwa kwa jina jipya ambalo Yahwe
atalichagua. [3] Pia utakuwa taji zuri katika mkono wa Yahwe, na kilemba cha ufalme

katika mkono wa Mungu wako. 4 Hautaambiwa tena, "Umetelekezwa"; wala kwa
nchi yako hautasema tena, "Ukiwa." kweli, itaitwa "Neema yangu iko kwake", na
nchi yao "ndoa" mana furaha ya Yahwe ndani yenu, na nchi yenu itaolewa. 5 Hakika,
kama kijana mdogo akimuoa mwanamke mdogo, hivyo watoto wako watawaoa ninyi,
na kama bwana harusi anavyofurahia juu ya bibi harusi, Mungu wenu atafuhai juu
yenu. 6 Nimemuweka mlinzi katika kuta zenu, Yerusalemu; hawatatulia mchana
wala usiku. Utabaki kuwa Yahwe, usitulie. 7 Usimuache apumzike mpaka ainzishe
tena Yerusalemu na kmfanya asifiwe duniani. 8 Yahwe ameapa kwa mkono wake
wa kuume na kwa mkono wa nguvu zake, "Hakika sitawapa tena nafaka kama
chakula cha maadui zenu. Wageni hawatakunjwa mvinyo wenu uliompya maana
mlifanya kazi. 9 Kwale watakao vuna nafaka watazila na kumsifu Yahwe, na wale
wanaochuma zabibu watakunjwa mvinyo katika mahakama ya madhebau yangu
takatifu." 10 Njooni pitieni, pitieni katika lango! Tenegenezeni mapito ya watu!
Itengenezeni, Tengeneza njia kuu! kusanyeni mawe! Nyanyueni juu ishara ya
bendera kwa mataifa! 11 Tazama, Yahwe ametangaza mwisho wa nchi, "Waambie
binti Sayuni: Tazama, Mkombozi wenu anakuja! Angalia, amebeba zawadi zake, na
malipo yake yapo mbele yake." 12 Watakuita wewe, "Mtu mtakatifu; Mkombozi wa
Yahwe," nawe utaitwa "Ulioacha kabla; mji usiotelekezwa."

# 63

1 Ni nani ajaye kutoka Edomu, aliyevaa mavazi rangi nyekundu kutoka Bozra?
Ni nani aliye katika mavazi ya kifahari, anayetembea kwa kujiamini kwa sababu
ya ukuu wa nguvu zake? Ndiye mimi, nizungumzae haki na uwezo mkubwa wa
kuokoa. 2 Kwa nini umevaa mavazi ya rangi nyekundu, na kwan nini wanaonekana
kama akanyagae mizabibu katika vyombo vyake. 3 Nimekanyaga zabibu lililoko
katika vyombo vyenyewe, na hakuna hata mmoja kutoka mataifa aliyeungana na
mimi. Niliwakanyaga kwa hasira yangu na niliwakanyaga wao kwa hasira yangu.
Damu zao zimeruka katika nguo zangu na kuweka madoa nguo zangu zote. 4 Maana
niliangalia mbele katika siku ya kisasi, na mwaka wa ukombozi ulikwishawadia.
5 Mimi nilitazama, na hapo hapakuwa na mtu mmoja hata wa kutoa msaada, lakini
mkono wangu mwenywe uliniletea ushindi mimi, na hasira yangu kubwa iliniongoza
mimi. 6 Niliwakanyaga watu wangu chini kwa hasira yangu na kuwafanya wao
wanywe laana yangu, na nilimwaga damu zao juu ya nchi. 7 Nitakusimulia matendo
ya agano la Yahwe lenye kuaminika, matendo ya kusifu ya Yahwe. Nitawasimulia
yote ambayo Yahwe ametutendea sisi, na ukuu wa uzuri wake katika nyumba ya
Israeli. Huruma hii aliyetuonyesha sisi kwa sababu ya rehema zake na matendo
ya agano lake la kuaminika. 8 Maana alisema, "Baadhi yao ni watu wangu, watoto
ambao sio waaminifu." Amekuwa mwokozi wao. 9 Kupitia mateso yao yote, aliteseka
pia, na malaika kutoka mbele yake aliwaokoa wao. Katika upendo wake na rehema
aliwakomboa wao, na aliwanyanyua juu na aliwabeba wote katika kipindi chote cha
kale. 10 Lakini walimuasi na kumuuzunisha roho mtakatifu. Hivyo basi akkawa
adui wao na kupigana dhidi yao. 11 Watu wake walifikiri kuhushu nyakati za kale
za Musa. Walisema, "Yuko wapi Mungu, aliyewaleta juu nje ya bahari pamoja na
mchungaji wa kundi lake? Yuko wapi Mungu, ambaye aliyeweka roho mtakatifu
mwiongoni mwenu? 12 Yuko wapi Mungu, aliyeufanya wingi wa utukufu wake
kwenda katika mkono wa kuume wa Musa, na ukaganya maji mbele yao, kulifanya
jina lake milele yeye mwenyewe? 13 Yuko wapi Mungu, aliyewaongoza katika maji
mengi? Kama farasi anayekimbia kwenye aridhi ambayo ni tambarare, hawakua
na mashaka. 14 Kama ng'ombe anayeshuka chini kwenye bonde, Roho ya Yahwe
imewapa punziko. Hivyo umewaongoza watu wako, kufanya wewe mwenyewe jina

la kusifu. [15] Tazama chini kutoka mbinguni na pata taarifa kutoka kwenye makao
ya utukufu wako. Iko wapi bidii yenu na matendo makuu? Uruatendo yako ya
uruma yamezuiliwaa kutoka kwetu. [16] Maana wewe n baba yetu, Japokuwa Ibrahimu
hatujui sisi, na Israeli haitutambui sisi, wewe, Yahwe, wewe ni baba yetu. Mkombozi
wetu limekuwa jina lako kutoka nyakati za kale. [17] Yahwe, kwa nini unatufanya
tangetange na kuifanya mioyo yetu kuwa migumu, hivyo hatukukuheshimu wewe?
Rudi kwa niaba ya watumishi wako, kabila la urithi wako. [18] Watu wako walirithi
mahali patakatifu kwa mda mfupi, halafu maadui zetu waliwakanyaga. [19] Tumekuwa
kama juu ya wale ambao hawajawai kuongoza, kama wale ambao hawajaitwa kwa
jina lako.

# 64

[1] "Oh, ikiwa umeigawa kwa kuifungua mbingu na kushuka chini! Milima inetikisika
mbele yako, [2] ni kama vile moto uunguzao vichaka, moto uchemshao maji. Oh,
jina lako lingejulikana kwa maadui wako, na ya kwamba mataifa yangetetemeka
mbele yako! [3] Awali, ulipofanya mambo ya ajabu ambayo hatukuyategemea,
ulishuka chini, milima ikatetemeka mbele zako. [4] Tangu nyakati za kale hakuna
hata mmoja aliyesikia au kujua, wala jicho kuona Mungu yeyote karibu yake, ni
nani afanyae mambo haya kwake anayemsubiri yeye. [5] Umekuja kuwasidia wale
wanaofurahia kutenda yaliyo ya haki, wale wanaowaita kuwakumbusha njia zake na
kumheshimu yeye. Ulipatwa na hasira tulipotenda dhambi. Katika njia zako daima
tutakombolewa. [6] Maana sote tumekuwa kama mmoja aliye na unajisi, na matendo
yetu ya haki yamekuwa kama hedhi kali. Sote tumenyauka kama majani; maovu
yetu, ni kama upepo, unaotupeperusha sisi mbali. [7] Hakuna hata mmoja anayeita
jina lako, hakuna anayefanya jitihada za kukushika wewe; maana umeuficha uso
wako mbali na sisi na kutufanya sisi kuwa takataka katika mkono wa maovu yetu.
[8] Na lakini, Yahwe, wewe ni baba yetu; sisi ni udongo. Wewe ni mfinyanzi wetu; sisi
ni kazi ya mkono wako. [9] Usiwe na hasira kubwa, Yahwe, wala daima usikumbuke
maovu dhidi yetu, tafadhali sisi sote, watu wako. [10] Miji yenu mitakatifu imekuwa
jangwa; Sayuni imekuwa jangwa, Yerusalemu imekuwa ukiwa. [11] Hekalu letu takatifu
na zuri. mahali ambapo baba zetu walikusifu wewe, limeangamizwa kwa moto, na
kila kilichokuwa karibu kiliharibiwa. [12] Je unawezaje kuendelea kumshika, Yahwe?
Unawezaje kutulia kimya na kuendelea kutufedhehesha sisi?"

# 65

[1] Nilikuwa tayari kuchaguliwa na wale ambao hawakuniomba; Nilikuwa tayari
kupatikana kwa wale ambao hawakunitafuta. Nilisema, "Niko hapa!' kwa taifa
ambalo halikuita jina langu. [2] Nimetawanya mikono yangu siku zote kuwasumbua
watu wangu, wanao tembea katika njia isiyopasa, wanaotembea kwa kufuata
mawazo yao wenyewe na mipango yao. [3] Kuna watu wanoendelea kunipinga mimi,
wanatoa sadaka zao katika bustani, na kuchoma ubani juu ya matofali. [4] Wamekaa
miongoni mwa makaburi na kuangalia usiku kucha, na hula nyama ya nguruwe
na mchuzi mchafu wa nyama katika vyombo vyao. [5] Wanasema, 'Simama mbali,
usisogee karibu na mimi, maana mimi ni mtakatifu zaidi yako.' Vitu hivi ni moshi
katika pua zangu, moto uwakao mchana kutwa. [6] Tazama, imeandikwa mbele
yangu: Sitanyamaza, Maana nitawalipa wao tena; nitafanya malipo yao katika
miguu yao, [7] kwa sababu ya dhambi zao na dhambi za baba zao kwa pamoja."
asema Yahwe. "Nitawajibu wao kwa kuchoma ubani juu ya milima na kunifanyia
mimi juu ya vilima. Hivyo basi nitapima juu ya matendo yao ya kale katika
miguu yao." [8] Yahwe asema hivi, "Ikiwa kama juisi itapatikana katika nguzo ya

zabibu, wakati mmoja ataposema, 'Usihiaribu hiyo, maa kuna uzuri ndani yake;
hichi ndicho nitakachokifanya kwa niaba ya watumishi wangu: Sitawaribu wao
wote. 9 Nitazileta koo kutoka kwa Yakobo, na kutoka Yuda wao ambao watairithi
milima yangu. Niliowachagua watairithi aridhi, na watumishi wangu wataishi pale.
10 Sharoni itakuwa malisho ya makundi, na bonde la Akori itakuwa sehemu ya
kupumzikia ya makundi yangu, kwa watu wangu wanaonitafuta mimi. 11 Lakini
yeye aliyeachana na Yehwe, anayeusahau mlima wangu mtakatifu, anayeandaa meza
kwa bahati ya mungu, na kujaza kikombe cha mvinyo uliochanganywa na miungu
inayoitwa Hatama. 12 Nitaufikisha mwisho wenu kwa upanga, na wato mtainama
chini kwa kuchinjwa, Kwa sababu nilipokuita wewe, haukuitikia; nilipozungumza
haukunisikliza. lakini mlifanya yaliyo mabaya katika macho yangu na kuchagua
kufanya yasiyo nipendeza mimi." 13 Bwana Yahwe asema hivi, "Tazama, mtumishi
atakula, lakini atashikwa na njaa; tazama mtumishi wangu atakunywa lakini
atakuwa na kiu; tazama mtumishi wangu atashangilia, lakini atatiwa katika aibu.
14 Tazama, mtumishi wangu atapiga kelele za furaha kwa sababu ya furaha ya moyo,
lakini utalia kwa sababu ya maumivu ya moyo, na mtapiga kelele kwa sababu ya
kusagwa kwa roho zenu. 15 Nanyi mtaliacha jina lenu nyuma kama laana kwa
watu niliowachagua wazungumze; Mimi Bwana Yahwe, Nitakuwa wewe; Nitawaita
watumishi wangu kwa jina lingine. 16 Yeyote atakaye tamka baraka juu ya nchi
atabarikiwa na mimi, Mungu wa kweli. Yeyote achukuae kiapo juu ya nchi anaapa
na mimi, Mungu wa kweli, kwa sababu matatizo ya nyuma yatasaulika, maana
yatafichwa machoni pangu. 17 Maana tazama, Ninakaribia kuumba mbingu mpya
na nchi mpya; na mambo ya kale hayatakumbukwa tena wala kufikiriwa katika
akili. 18 Lakini mtakuwa na furaha na kushangilia daima kwa nitakachokiumba.
Tazama, Ninakaribia kuumba Yerusalemu mpya kama furaha na watu wake wenye
furaha. 19 Nitafurahia juu ya Yerusalemu watu wangu; kuomboleza na kilio cha dhiki
akitasikika tena ndani yake. 20 Hakuna tena mtoto atakayeishi pale japo kwa siku
chache; wala mzee kufa kabla ya mda wake. Yule atakayekufa katika umri wa miaka
mia moja atachukuliwa kama mtu mdogo. Yeyote ambaye atashindwa kufikia umri
wa miaka mia moja atachukuliwa kama laana. 21 Watazijenga nyumba na kukaa
huko, na watapanda mizabibu na kula matunda yake. 22 Hawatajenga nyumba na
wengine waishi humo; hawatapanda, na wengine wale; maana kama siku za miti
zitakuwa siku za watu wangu. Watu wangu wataishi kikamilifu kwa kazi ya mikono
yao. 23 Hawatafanya kazi bure, wala kuzaa kwa kusikitishwa. Maana ni watoto wa
waliobarikiwa na Yahwe, pamoj na koo zao. 24 Kabla hawajaita, nitaitika; na wakati
wanaendele kuzungumza, ntisikia. Mbwa mwitu na kondoo watachungwa pamoja,
na simba atakula majani kama ng'ombe; lakini udongo utakuwa chakula cha nyoka.
25 Hawataumiza tena wala kuharibujuu ya mlima wangu mtakatifu," asema Yahwe.

# 66

1 Yahwe asema hivi, "Mbinguni ni makao yangu, na nchi ni miguu yangu. Iko
wapi nyumba uliyonitengenezea mimi? iko wapi sehemu amabayo ninaweza
kupumzika? 2 Mkono wangu umeyafanya haya yote; hivi ndovyo jinsi ambavyo
vitu vitatokeavyo—hili ndilo tamko la Yahwe. Mtu niliyempitisha, mwenye roho
iliyopondeka na mwenye kujutia roho, na atetemekaye kwa ajili ya neno langu.
3 Yeyote achinjae ng'ombe humuua mtu pia; yeye anayetoa sadaka ya kondoo
huvunja shingo ya mbwa pia; yeye anayetoa sadaka ya mavuno anatoa sadaka
ya damu yangurue; yeye anayetoa kumbukumbuvumba huwabariki wakosaji pia.
Wamechagua njia zao wenyewe wanachukua radhi kwa uchafu wao wenyewe.

4 Katika njia hiyo hiyo nitachagua adhabu yao wenyewe; Nitaleta juu yao kitu wana-
chokiogopa, maana niilpowaita, hakuna aliyeitika; nilipozungumza aliyenisikiliza
mimi. Walifanya yaliyo maovu mbele yangu, na kuchagua yasiyo nipenindeza mimi.''
5 Sikiliza neno la Yahwe, ewe utemekae kwa neno lake, ''Kaka zako wanaonichukia
na kukutenga wewe kwa ajili ya jina langu walisema, 'Na atukuzwe Yahwe, halafu
tutaiona furaha yenu; lakini mtatiwa katika aibu. 6 Sauti ya vita vya ghasi vinakuja
katika mji, sauti kutoka hekaluni, sauti ya Yahwe anawarudia maadui zake. 7 Kabla
ajaenda katika chumba, hujifungua; kabla ya uchungu kumtoka hujifungua mtoto
wa kiume. 8 Ni nani asikiaye mambo haya? Ni nani aonae mambo haya? Je taifa
linaweza kuanzishwa kwa wakati mmoja? lakini kwa haraka Sayuni inapokwenda
katika chumba, hujifungua watoto wake. 9 Ninawezaje kumleta mtoto azaliwe na
nisimruhusu mtoto azaliwe? Yahwe auliza? — au Je ninamleta mtoto wakati tu wa
kujifungua na halafu nimshikilie tena - anauliza Yahwe.'' 10 Furahia na Yerusalemu
na fuhahia kwa ajili yake, ninyi nyote mnaopenda yeye; furahia pamoja na yeye,
ninyi mnaomboleza juu yake! 11 Maana utamuuguza na ataridhika, katika maziwa
yake atakufariji; utakunywa mpaka ushibe na kufurahia kwa wingi wa utukufu wake.
12 Yahwe asema hivi, ''Ni nanakaribia kutawanya mafanikio juu katika mto, na utajiri
wa mataifa kama wingi wa mkondo wa maji. Utamuuguza kwa upande wake, na
kubebwa katika mikono yake, mtabebwa juu ya magoti yake. 13 Kama vile mama
anavyomfariji mtoto wake, hivyo basi nami nitawafariji ninyi, na mtapata faraja
katika Yerusalemu.'' 14 Utayaona haya, na moyo wako utafurahia, na mifupa yako
itachipukia kama zabuni ya nyasi. Aridhi ya Yahweitajulikana kwa watumishi wake,
lakini atawaonyesha hasira yake dhidi ya maadui zake. 15 Kwa kutazama, Yahwe
anakuja kwa moto, na gari lake linakuja kama upepo wa dhoruba kuleta joto katika
hasira yake na kukemea kwake ni kama moto uwakao. 16 Maana Yahwe ametekeleza
hukumu juu ya watu kwa moto na kwa upanga wake. Wale watakaouliwa na Yahwe
watakuwa wengi. 17 Watajiweka wakfu wenyewe na kujisafisha wenywe, ili waweze
kuingia katika bustani, kumfuata aliyeko katikati ya wale walao nyama ya nguruwe
na vitu haramu kama panya. ''Watafika mwisho - hili ni tamko la Yahwe. 18 Maana
ninayajua matendo yao na mawazo yao. Wakatiutafika nitakapoyakusanya mataifa
yote na lugha zote. Watakuja na kuona utukufu wangu. 19 Nitaweka ishara ya
ukuu wangu miongoni mwao. Halafu nitawatuma wakazi kutoka miongoni mwao
kwa mataifa. Kwa Tarshishi, Puti, na Ludi, upinde wale wanaochukua upinde wao,
kwa Tubali, Javani, na umbali kuelekea katika pwani kule ambapo hawajasikia
chochote kuhusu mimi wala kuona utukufu wangu. Watatangaza utukufu wangu
miongoni mwa mataifa. 20 Watawaleta kaka zako wote nje ya mataifa yote, kama
sadaka kwa Yahwe. Watakuja kwa farasi na kwa gari, na kwa gari, juu ya nyumbu
na juu ya ngamia, kuelekea mlima wangu mtakatifu Yerusalemu - asema Yahwe.
Maana watu wangu wa Israeli wataleta sadaka ya mavuno kwenye vyombo visafi
katika nyumba ya Yahwe. 21 Baadhi ya vitu hivi nitavichagua kama makuhani na
walawi — asema Yahwe. 22 Maana itakuwa mbingu mpya na nchi mpya ambayo
nitakayoifanya ibaki mbele zangu— Hili ndilo tamko la Yahwe— Hivyo ndivyo
ukoo wenu utakavyobakia, na jina lenu litabaki. 23 Kutoka mwenzi mmoja mpaka
mwingine, na kutoka sabato moja mpaka nyingine, watu wote watakuja kukuinamia
chini— asema Yahwe. 24 Watakwenda nje na kuona miili ya wafu ya watu walioniasi
mimi, maana wadudu wawalao wao hatakufa, na moto huwaunguzao hautazimika;
na itakuwa ni chuki kwa wale wote wenye mwili.''

# Yeremia

1 Hili ndilo neno la Yeremia mwana wa Hilikia; yeye alikuwa mmoja wa makuhani
kule Anatothi katika nchi ya Benjamini. 2 Neno la BWANA lilimjia katika siku za
Yosia mwana wa Amoni, mfalme wa Yuda, katika mwaka wa kumi na tatu wa
utawala wake. 3 Lakini pia lilimjia katika wakati wa Yehoyakimu mwana wa Yosia,
mfalme wa Yuda, mpaka mwezi wa tano wa mwaka wa kumi na moja wa Zedekia
mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda, wakati watu wa Yerusalemu walipochukuliwa
kuwa watumwa. 4 Neno la BWANA lilinijia, likisema, 5 “kabla sijakuumba tumboni,
Nilikuchagua; kabla hujazailiwa toka tumboni Nilikutenga; Nilikufanya kuwa nabii
kwa mataifa.” 6 “Ahaa, BWANA!” Nilisema, “mimi sijui kusema, kwa kuwa mimi ni
mtoto.” 7 Lakini BWANA akaniambia, “Usiseme, 'mimi ni mtoto.' Utaenda kila mahali
ninapokutuma, na utasema kila kitu ninachokuamuru! 8 Usiwaogpe hao, kwa kuwa
Mimi niko pamoja na wewe kukuokoa- asema BWANA.” 9 Kisha BWANA akanyosh
mkono wake, akagusa kinywa changu, na akaniambia, “Nimeweka maneno yangu
kinywani mwako. 10 Nimekuchagua leo juu ya mataifa na juu ya mataifa, ili kung'oa
na kuvunja, kuharibu na kutupa, kujenga na kupanda.” 11 Neno la BWANA lilinijia,
likisema, “Yeremia, unaona nini?” Nikasema, “Ninaona tawi la mlozi.” 12 BWANA
akaniambia, “umeona vyema, kwa kuwa ninaliangalia neno langu ili nilitimize.”
13 Neno la BWANA likaniji mara ya pili likisema, “Unaona nini? “Nikasema, “Ninaona
chungu kikichemuka, ambacho mdomo wake unaelekea toka upande wa kaskazini,”
14 BWANA akaniambia, “Janga litatokea kaskazini juu ya wote wanaoishi katika nchi
hii. 15 Kwa kuwa ninayaita makabila yote ya falme za kaskazini, asema BWANA.
Yatakuja, na kila mmoja atasimika enzi yake katika malango ya Yerusalemu, dhidi ya
kuta zote zinazoizunguka, na dhidi ya miji ya Yuda. 16 Nitatamka hukumu dhidi yao
juu ya uovu wao wa kuniacha, kwa kufukiza uvumba kwa miungu mingine, na kwa
kuabudu kile walichotengeneza kwa mikono yao. 17 Jiandae! Simama ukawaambie
kila kitu ninachokuamuru. Usifdhaike mbele zao nisije nikakufadhaisha wewe mbele
zao! 18 Tazama! Leo nimekufanya kuwa mji ulio na ngome, kuwa ngome ya chuma,
na ukata wa shaba dhidi ya nchi yote - dhidi ya wafalme wa Yuda, na juu ya wakuu
wake, na juu ya makuhani wake, na juu ya watu wote wa nchi. 19 Watapigana na
wewe, lakinai hawatakushinda, kwa kuwa nitakuwa pamoja na wewe ili kukuokoa-
asema BWANA.”

## 2

1 Neno la BWANA lilinijia likisema, 2 “Nenda ukanene katika masikio ya
Yerusalemu. Useme; BWANA asema hivi: Ninakumbuka agano la uaminifu la ujana
wako, upendo wako wakati tulipokuwa tumechumbiana, ulipokuwa ukinihitaji kule
jangwani, katika ile nchi iliyokuwa haijapandwa. 3 Israeli alikuwa ametengwa
kwa BWANA, malimbuko yake ya mavuno yake! Wote waliokula malimbuko yake
walikuwa na hatia! majanga yaliwajia—asema BWANA.'” 4 Sikilizeni neno la BWANA,
enyi nyumba ya Yakobo na kila familia katika nyumba ya Israeli. 5 BWANA anasema
hivi, “Ni makosa gani ambayo baba zenu waliyaona kwangu, hata wakatae kunifuata
mimi? hata wazifuate sanamu ambazo hazina chochote na wao kuwa si kitu? 6 Wala
hawakusema, BWANA yuko wapi, ambaye alitutoa katika nchi ya Misri? BWANA
yuko wapi, ambaye alituongoza katika jangwa, katika nchi ya Araba na mashimo,
katika nchi ya ukame na giza nene, katika nchi ambayo hakuna mtu apitaye wala
hakuna mtu anayeishi humo? 7 Lakini nilwaleta katika nchi ya Kameli, ili mle
matunda yake na vitu vingine vyema! Lakini mlipokuja, mliitia unajisi nchi yangu,

mliufany urithi wangu kuwa chukizo! 8 Hata makuhani hawakusema, 'BWANA
yuko wapi?' na watalamu wa sheria hawakunijali mimi! wachungaji wametenda
dhambi dhidi yangu. Manabii wamemtolea Baali unabii na kuvitafuta vitu ambvyo
havina faida. 9 Kwa hiyo nitaendelea kuwashitaki - hili ni neno la BWANA - na
nitawashitiki watoto wa watoto wenu. 10 Kwa kuvuka kwenda hadi pwani ya Kitimu
na kutazama. Tuma wajumbe kwenda Kedari na tafuta uone kama kama iliwahi
kutokea hapo awali vitu kama hivi. 11 Je, taifa limebadilisha miungu, hata kama
haikuwa miungu? Lakini watu wangu wameubadili utukufu wao kwa kitu ambacho
hakiwezi kuwasaidia. 12 Sitajabuni, enyi mbingu kwa sababu ya hili! Tetemekeni
na kuogopa -asema BWANA. 13 Kwa kuwa watu wangu wametenda maovu mawili
dhidi yangu: Wameziacha chemichemi za maji ya uhai kwa kuchimba mabarika kwa
ajili yao, mabarika yanayovuja yasiyoweza kutunza maji! 14 Je, Israeli ni mtumwa?
Kwani hakuzaliwa nyumbani? Kwa nini sasa amekuwa nyara? 15 Wanasimba
wameunguruma dhidi yake. Wamepiga kelele sana na kuifanya kuwa ukiwa.
Miji yake imeharibiwa na kubaki bila watu. 16 Pia watu wa Nufu na Tahapanesi
watakinyoa kichwa chako. 17 Je, hamkufanya haya kwa ajili yenu mlipomwacha
BWANA, wakati Mungu wenu, alipokuwa akiwaongoza njiani? 18 Kwa hiyo, kwa
nini kutafuta msaada Misri na kunywa maji ya Shihori? Kwa nini kutafuta msaada
Ashuru na kunywa maji ya Mto Frati? 19 Uovu wako unakukemea, na maasi yako
yatakuadhibu. Kwa hiyo yafikiri hayo; tambua kuwa ni uovu na uchungu kwenu
ninyi kuniacha mimi, BWANA Mungu wako, na kutokuwa na hofu yangu - asema
BWANA wa majeshi. 20 Kwa kuwa niliivunja nira yenu mliyokuwa nayo wakati wa
kale; Nilivichana vifungo vyako kutoka kwako. Lakini bado ulisema, 'Sitamtumikia!'
tangu ulipopiga magoti katika kila kilima kuusogelea kila mti wenye majani mabichhi,
enyi makahaba. 21 Lakini mimi mwenyewe niliwapanda kama mzabibu niliouchagua,
mbegu iliyokamilika. Lakini tazama jinsi ulivyobadilika mbele yangu, na kuwa
mzabibu usiofaa na mzabibu pori! 22 Kwa kuwa hata kama utajisafisha mwenyewe
mtoni na kuoga kwa sabuni kali, bado dhambi yako ni madoa mbele yangu - asema
BWANA Mungu. 23 Wawezaje kusema, 'Mimi sijanajisika! Mimi sjaenda kwa Mabaal?'
Tazama tabia zako zilivyokuwa bondeni! Tambua kile ulichofanya, wewe ngamia
mwepesi! akimbiaye katika njia yake! 24 Wewe ni punda wa mwitu, aliyeizoelea
nyika, avutaye pumzi za upepo usiofaa katika tamaa ya kuishi! Ni nani awezaye
kumgeuza anapotafuta dume la kumpanda? Na punda dume amtafutaye hajichoshi
mwenyewe. Huenda kwake wakati wa mwezi wa kupandwa. 25 Lazima uizuie
miguu yako isikose kiatu na koo lako kuwa na kiu! Lakini umesema, 'Hakuna
matumaini! Hapana! Nawapenda wageni nami huwatafuta!' 26 Kama aibu ya mwizi
ilivyo anapokuwa amekamatwa, ndivyo aibu ya Israeli itakavyokuwa - wao, wafalme
wao, malikia wao, makuhani na manabii wao! 27 Hawa ndio wale waiambiayo
miti, 'Ninyi ndio baba zangu,' na mawe, 'Ninyi ndio mlinizaa.' Kwa kuwa migongo
yao hunitazama na siyo nyuso zao. Hata hivyo, wakati wa shida husema, 'Amka
utuokoe!' 28 Lakini iko wapi ile miungu mliyojitengenezea? Acha hao wainuke kama
wanaweza kuwaokoa wakati wa shida, kwa kuwa hizo sanamu zenu zina idadi
sawa na miji yenu, katika Yuda. 29 Kwa hiyo kwa nini kunituhumu kwa kufanya
makosa? Ninyi nyote mmeniasi - asema BWANA wa majeshi. 30 Nimewadhibu watu
wenu bure. Wala hawakutaka kurudiwa. Upanga wako umewaangamiza manabii
wenu kama kama simba aangamizaye! 31 Enyi watu wa kizazi hiki! Sikilizeni neno
langu, neno la BWANA! Je, nimekuwa jangwa kwa Israeli? Au nchi yenye giza nene?
Kwa nini watu wangu husema, 'Acha tuzungukezunguke, hatutakuja kwako tena'?
32 Je, mwanamwali anaweza kusahau mapambo yake, na bibi arusi mavazi yake?
Lakini watu wngu wamenisahau mimi kwa siku nyingi! 33 Jinsi mlivyotengeneza

njia zenu vizuri ili kutafuta mapenzi. Hata mmewafundisha njia zenu wanawake
waovu. 34 Damu ambayo ilikuwa ndio uhai wa watu wasio na hatia, imeonekana
katika mavazi yenu. Hawa watu hawajawahi kuonekana katika matendo maovu.
35 Pamoja na mambo haya yote, wewe unaeendelea kusema kuwa hauna hatia. Kwa
hakika hasira ya BWANA itageuka kutoka kwangu. 'Lakini tazama! Utahukumiwa
kwa sababu, 'Sikutenda dhambi.' 36 Kwa nini mnatangatanga kwa urahisi katika njia
zenu? Pia Misri itawahuzunisha sana, kama ilivyokuwa kwa Ashuru. 37 Mtaondoka
hapo mkiwa mmehuzunika sana, mkiwa mmeweka mikono vichwani mwenu, kwa
kuwa BWANA amemkutaa yule mliyemtumainia, kwa hiyo hamtapata msaada toka
kwao,”

# 3

1 Wanaema, 'Mwanamume akimfukuza mke wake, naye akaondoka kwake na
kuwa mke wa mwanamume mwingine. Je, anaweza kumrudia tena? Je huyo si
najisi kabisa?' Huyo mwanamke ndiyo hii nchi! Mmetenda kama kama Kahaba
aliye na wapenzi wengi, na sasa mnapenda kurudi kwangu tena? - asema BWANA
wa majeshi. 2 Inua macho yako uvitazame vielele tasa! Je kuna mahali ambapo
hukufanya ukahaba? Pembeni mwa barabara ulikaa ukisubiri wapenzi wako, kama
vile Mwarabu jangwani. Uneiharibu nchi kwa ukahaba na uovu wako. 3 Kwa hiyo
chemichemi za mvua zilizuiliwa na mvua za vuli hazikunyesha. Lakini uso wako una
kiburi, kama uso wa mwanamke kahaba. Unakataa kuona aibu. 4 Na sasa hutaniita
mimi: 'Baba yangu, hata marafiki zangu wa tangu ujanani! Je, atakuwa na hasira
dhidi yangu milele? 5 Je, utaendelea kuwa na hasira zako?' Tazama! Umesema
kuwa utatenda maovu, na kweli umetenda hivyo. kwa hiyo endelea kufanya hivyo!”
6 Kisha BWANA akanena nami katika siku za mfalme Yosia, “Je, unaona jinsi Israeli
alivyoniasi? Yeye anaenda kwenye kila kilima na katika kila mti wenye majani
mabichi, na kule anafanya kama mwanamke kahaba. 7 Nikisema, 'Baada ya kuwa
amefanya mambo haya yote, atanirudia,' lakini hakurudi. Kisha dada yake Yuda
ambaye ni mwasi pia aliona alichokifanya. 8 Kwa hiyo nami nikaona kuwa kwa
sababu amefanya uzinzi huu wote. Huyo Israeli aliyeasi! Nilimfukuza na kumpatia
talaka ya ndoa. Lakini dada yake Yuda mwenye hiana hakuwa na hofu, na yeye
akaenda kuafanya kama mwanamke kahaba! 9 Hukusikitika kuwa ameinajisi nchi,
kwa hiyo wakatengeneza sanamu za mti na za jiwe. 10 Kisha baada ya haya yote,
wala Yuda dada yake muasi hakurudi kwangu na moyo wake wote, bali alikuja na
uongo! -asema BWANA wa majeshi,” 11 Kisha BWANA akanena na mimi, “Israeli
muasi amekuwa mwenye haki zaidi kuliko Yuda muasi! 12 Nenda ukaseme maneno
haya huko kaskazini. Uwaambie, 'Rudi wewe Israeli uliyeasi! - asema BWANA -
sitakuwa na hasira dhidi yako. Kwa kuwa mimi ni mwaminifu - asema BWANA -
sitakuwa na hasira milele. 13 Kiri uovu wako, kwa kuwa umefanya dhambi dhidi
ya BWANA, Mungu wako; umemshirikisha njia zako mgeni chini ya kila mti wenye
majani mabichi! wala hukuisikiliza sauti yangu! - asema BWANA. 14 Rudini, enyi
watu waasi! - asema BWANA - kwa kuwa mimi nimekuoa wewe! Nitakurudisha
wewe mmoja katika mji, wawili katika ukoo mmoja, na nitawarudisha Sayuni!
15 Nitawapa wachungaji niwapendao, na watawachunga kwa maarifa na ufahamu.
16 Ndipo itakapotokea kuwa utaongezeka na kuzaa matunda katika nchi hiyo siku
hizo-asema BWANA. Hawataweza kusema kuwa, “Sanduku la agano la BWANA!
Jambo hili hawatalikumbuka tena katika mioyo yao, kwa kuwa hawataliwaza tena
wala kulijali tena. Usemi huu hawatausema tena.' 17 Katiak wakati huo watasema juu
ya Yerusalemu, 'Hii ndiyo enzi ya BWANA,' na mataifa mengine yote yatakusanyika
Yerusalemu katika jna la BWANA. Hawataishi katika taabu ya uovu wa mioyo

yao. 18 Katika siku hizo, nyumba ya Yuda itaishi na nyumba ya Israeli. Watarudi
pamoja kutoka katika nchi ya kaskazini katika nchi niliyowapa mababu wao kuwa
urithi. 19 Lakini mimi, Nilisema, 'Jinsi nipendavyo kukuheshimu kama mwanangu
na kukupa nchi ipendezayo, kuwa urithi mzuri kuliko ulio katika taifa lolote!' Nami
nikasema, ''mtaniita baba yangu''.'Nami nitasema kwamba hamtageuka na kuacha
kunifuata. 20 Lakini kama mwanamke aliyemwasi mume wake, mmenisaliti, enyi
nyumba ya Israeli - asema BWANA." 21 Sauti ilisikika juu ya nyanda, kilio na kusihi
kwa watu wa Israeli! kwa kuwa wamezibadili njia; wamemsahau BWANA, Mungu
wao. 22 "Rudini enyi watu mlioasi! Nami nitawaponya na uasi wenu!" "Tazama!
tutakuja kwako, kwa kuwa wewe ni BWANA, Mungu wetu! 23 Uongo hutoka kwenye
vilima, kutoka kwenye milima mingi. Kwa hakika wokovu wa Israeli unapatikana
kwa BWANA, Mungu wetu. 24 Lakini miungu ya aibu imeramba kazi ambayo mababu
zetu waliifanya - makundi yao ya kondoo na ng'ombe, wana wao na binti zao! 25 Na
tulale chini kwa aibu. Aibu yetu na itufunike, kwa kuwa tumefanya dhambi dhidi ya
BWANA, Mungu wetu! Sisi wenyewe na mababu zetu, kutoka wakati wa ujana wetu
hadi leo, hatujaisikiliza sauti ya BWANA, Mungu wetu!"

# 4

1 "Kama utarudi, Israeli- asema BWANA - ikawa kwangu kwamba umerudi. Kama
utaondoa hayo mambo yachukizayo mbele yangu na ukaacha kunikimbia mimi tena,
2 na ukaapa hivi, 'kama BWANA aishivyo katika kweli, na haki, na katika hukumu.'
mataifa yataniomba baraka, na yatanisifu mimi. 3 Kwa kuwa BWANA asema hivi kwa
kila mmoja katika Yuda na Yerusalemu; 'Limeni shamba zenu na msipande katika
miiba. 4 Mtahiriwe kwa BWANA na kuondoa govi za mioyo yenu, ninyi wanaume
wa Yuda na wakazi wa Yerusalemu, vinginevyo hasira yangu itawaka kama moto
na kuteketeteza, na hakutakuwa na mtu wa kuizima. Hii itatokea kwa sababu ya
uovu wa matendo yenu. 5 Waambie Yuda na Yerusalemu isikie. Waambie, "pigeni
baragumu katika nchi." Tangazeni, "Kusanyeni pamoja. Twendeni kwenye miji ya
Maboma." 6 Inueni ishara za bendera na zielekezeni Sayuni, na kimbilieni usalama!
Msibaki, kwa kuwa ninaleta majanga kutokea kaskazini na anguko kubwa. 7 Simba
anakuja kutokea kwenye kichaka chake na yeye atakayeyaharaibu mataifa ameanza
kuja. Anaondoka kwenye eneo lake ili aache hofu katika nchi yenu, kuibadili miji
yenu kuwa uharibifu, ambapo hakuna hata mmoja atakayeishi. Kwa sababu hii vaeni
magunia, lieni na kuomboleza. 8 Kwa kuwa nguvu ya hasira ya BWANA haijaondoka
kwetu. 9 Ndipo itakapotokea katika siku hiyo - asema BWANA - mioyo ya mfalme
na wakuu itakufa. Makuhani watasitaajabu na manabii watashangaa.'" 10 Kwa hiyo
nikasema, "Ahaa! BWANA. Kwa hakika umewadanganya watu hawa na Yerusalemu
kwa kuwaambia, 'Kutakuwa na amani kwenu.'Wakati upanga unawaangukia dhidi
ya maisha yao." 11 Wakati huo itasemwa juu ya mji huu na Yerusalemu kuwa,
"Upepo uwakao kutoka katika nyanda za jangwani utachukua njia yake kuelekea
kwa binti ya watu wangu. Hautapepetwa wala kuwatakasa. 12 Upepo ulio na nguvu
sana utakaokuja kwa amri yangu, na sasa nitapitisha hukumu dhidi yao. 13 Tazama
anavamia kama wingu, na magari yake ni kama dhoruba. Farasi wake wana mbio
kuliko tai. Ole wetu kwa kuwa tutaharibiwa! 14 Itakaseni mioyo yenu kutoka uovu
wenu, Yerusalemu, ili kwamba muokolewe. Mawazo yako mabaya yatafikiri juu ya
kutenda dhambi mpaka lini? 15 Kwa kuwa kuna sauti iletayo habari kutoka Dani,
na janga lijalo linasikika kutoka vilele vya milima ya Efraimu. 16 Yafanyeni mataifa
kulifikiria hili: Tazama, na uwatangazie Yerusalemu kuwa wale watekaji wanakuja
kutoka katika nchi ya mbali ili kupiga kelel za vita juu ya miji ya Yuda. 17 Watakuwa
kama walinzi wa shamba liliolimwa dhidi yake pande zote, kwa kuwa amekuwa

mpinzani wangu - asema BWANA - 18 tabia na matendo yako yamesababisha haya
yatokee kwako. Hii itakuwa adhabu yako. Jinsi itakavyokuwa vibaya kwako!
itakupiga moyo wako. 19 Moyo wangu! Moyo wangu! Niko katika maumivu ya moyo.
Moyo wangu umefadhaika ndani yangu. Siwezi kunyamaza kwa kuwa nasikia sauti
za pembe, sauti za vita. 20 Anguko baada ya anguko limetangazwa, kwa nchi yote
imeharibika mara. Wanaharibu masikani yangu na hema yangu ghafula. 21 Vita hivi
vitaendelea mpaka lini? Ni mpaka lini nitasikiliza sauti za pembe? 22 Kwa kuwa
upumbavu wa watu wangu - hawanijui mimi. Ni watu wajinga wasio na ufahamu.
Wanaufahamu wa mambo maovu, tena hawajui kutenda mema. 23 Niliiona nchi,
na kuiona! ilikuwa ukiwa na utupu. Kwa kuwa hapakuwa na taa za mbinguni.
24 Nilitazama katka miliima. Tazama, ilikuwa inatetemeka, na vilima vyote vilikuwa
vinatikisika. 25 Nilitazama. Tazama, hapakuwa na mtu, na ndege wote wa angani
walikuwa wamekimbia. 26 Nikaangalia. Tazama, mashamba yalikuwa jangwa na
miji imeangushwa mbele za BWANA, mbele ya hasira yake.” 27 Hiki ndicho BWANA
asemacho, “Nchi yote itakuwa uharibifu, lakini sitawaharibu wote kabisa. 28 Kwa
sababu hii nchi itaomboleza, na mbingu juu zitatiwa giza. Kwa kuwa nimesema
haya na kuyakusudia; sitarudi nyuma; Sitaacha kuyatekeleza. 29 Kila mji utakimbia
kutoka katka kelele za wapandafarasi na wenye pinde; Watakimbilia msituni, Kila
mji utapanda hadi mahali pa miamba. Miji itatelekezwa, kwa kuwa hakutakuwa
na mtu wa kuishi katika miji hiyo. 30 Sasa umeharibiwa, utafanya nini? Japokuwa
unavaa mavazi mekundu, unajipamba na mapambo ya dhahabu, na kuyafanya
macho yako yaonekane makubwa na kupakwa wanja, wale wanaume waliokutamani
sasa wanakukataa. Badala yake wanajaribu kukuua. 31 Kwa hiyo nasikia sauti ya
maumivu, yenye utungu kama ya mwanamke azaaye mtoto wake wa kwanza, sauti
ya binti wa Sayuni. Atwetaye kupata pumzi. Ananyosha mikono yake na kusema,
'Ole wangu mimi! ninazimia kwa sababu ya wauaji hawa.'”

# 5

1 Kimbieni mkapite katika mitaa ya Yerusalemu, Tafuteni katika viwanja vyake.
Kama mtaweza kumpata hata mtu mmoja anayetenda kwa haki na kufanya kwa
uaminifu, basi nitaisamehe Yerusalemu. 2 Hata kama wanasema, 'Kama BWANA
aishivyo,' wanaapa uongo.” 3 BWANA, macho yako hayatazami uaminifu? Unawapiga
watu, lakini hawasikii maumivu. Umewaangsmiza kabisa, lakini bado wanakataa
kuwa waadilifu. Wanafanya nyuso zao kuwa ngumu kama mwamba. kwa kuwa
wanakataa kutubu. 4 Kwa hiyo nilisema, “Hakika hawa ni watu masikini, Ni
wapumbavu, Kwa kuwa hawazijui njia za BWANA, wala maagizo ya Mungu wao.
5 Nitaenda kwa watu wa muhimu na kutangaza ujumbe wa Mungu kwao, kwa
kuwa angalau wanazijua njia za BWANA, maagizo ya Mungu wao. Lakini wote
wanavunja nira yao pamoja; wote wanaivunja ile minyororo inayowafunga kwa
ajili ya Mungu. 6 Kwa hiyo simba kutoka mwituni atawavamia. Mbweha kutoka
Arabaha atawaangamiza. Chui ataivunja miji yao. Mtu yeyota anayeenda nje ya
mji wake atavunjwavunjwa. Kwa kuwa maovu yao yameongezeka. Matendo yao ya
uasi hayana ukomo. 7 Kwa nini niwasamehe hawa watu? Wana wenu wameniacha
na wamefanya viapo na wale ambao si miungu. Niliwalisha vya kutosha, lakini
wamefanya uasherati na kuchukua alama za nyumba ya uzinzi. 8 Walikuwa farasi
wanaotafuta kupandwa. Walitembea huku na huku wakitafutwa kupandwa. Kila
mwanamume alimkaribia mke wa jirani yake. 9 Kwa hiyo kwa nini nisiwaadhibu -
asema BWANA - na kwa nini nisijilipizie kisasi juu ya taifa kama hili? 10 Nenda hadi
kwenye kuta za shamba lake la mizabibu na zihariibuni. Lakini wao msiwaharibu
kabisa. Ondoeni matawi kwa sababu hayatoki kwa BWANA. 11 Kwa sababu nyumba

ya Yuda na Israeli wamenisaliti kabisa - asema BWANA - 12 na wamenikataa.
Wanasema, ''Yeye si halisi. Maovu hayawezi kutupata, wala hatutaona upanga wala
njaa. 13 Kwa kuwa manabii wamekuwa si kitu kama upepo na hakuna mtu mwiingine
wa kunena ujumbe wa BWANA kwetu. Vitisho vyao na viwjie wao wenyewe."' 14 Kwa
hiyo BWANA, Mungu wa majeshi asema hivi, tazama nataka kuweka maneno yangu
katika kinywa chako. Yatakuwa kama moto na watu hawa watakuwa kama kuni!
Kwa kuwa utawaramba. 15 Tazama nataka kuleta taifa dhidi yenu kutoka mbali,
enyi nyumba ya Israeli - asema BWANA - ni taifa linalodumu, taifa la kale! Ni taifa
ambalo lugha yake hamuijui, wala hamtaelewa wasemacho. 16 Podo lao ni kaburi
wazi. Wote ni wanajeshi. 17 Kwa hiyo mavuno yako yataliwa, wana wako na binti
zako pia, na chakula chako. Watakula kondoo wako na ng'ombe wako, watakula
matunda ya zabibu zako na ya mitiini. Wataiangusha chini miji yenu na boma zake
ambazo mnazitumainia. 18 Lakini hata katika siku hizo - asema BWANA - sikusudii
kuwaharibu kabisa. 19 Itatokea kwenu, ninyi Yuda na Israeli, mkisema, 'Kwa nini
BWANA, Mungu wetu ametufanyia haya yote?' kwamba wewe Yeremia, utawaambia,
'Kama vile mlivyomwacha BWANA na kuabudu miungu mingine katika nchi yenu,
vivyo hivyo mtawatumikia wageni katika nchi ambayo si yenu.' 20 Waambia haya
watu wa nyumba ya Yakobo na yasikike katika Yuda. Waambie, 21 'Sikilizeni hili,
eny watu wapumbavu! Sanamu hazina matakwa; zina masikio lakini haziwawezi
kusikia. 22 Je, hamnihofu mimi - asema BWANA - au kutetemeka mbele ya uso wangu?
Nimeweka mpaka wa mchanga kwenye bahari, ambao ni agizo la kudumu ambalo
halibomoki - hata kama bahari ina kupwa na kujaa, bado hauwenzi kubomoka. Hata
kama mawimbi yake yanaunguruma, hayawezi kuvuka. 23 Lakini hawa watu wana
mioyo ya usumbufu. Hugeuka kuwa wapinzani na kuondoka. 24 Kwa kuwa hawasemi
mioyoni mwao, "basi na tumche BWANA, Mungu wetu, yeye aletaye mvua za awali
na mvua za vuli - kwa wakati wake, ambaye hutuzna majuma ya mavuno kwa ajili
yetu." 25 uovu wako umezuia haya yasitokee. Dhambi zako zimeyazuia mambo
mema yasitokee. 26 Kwa watu waovu wamo kati ya watu wangu. Wanatazama
kama mtu anayenyatia ili kukamata ndege; wanaweka mitego na kukamata watu;
27 Kama tundu la mtego lijaavyo ndege, nyumba zao zimejaa uongo. Kwa hiyo
wanakua na kutajirika. 28 Wamenenepa; wanang'aa na kupendeza. Wamepitiliza
hata mipika ya maovu. Wala hawajali sababu ya kuwepo kwa watu na wala uwepo
wa yatima. Wanafanikiwa hata kama hawatoi hukumu ya haki kwa yatima. 29 Kwa
nini nisiwadhibu kwa sababu ya haya - asema BWANA - sitajilipizia kisasi juu ya
taifa la namna hii? 30 Jambo la ajabu na la kuchukiza limetokea katika nchi hii.
31 Mananbii wanatabiri kwa uongo, na makuhani wanatwala kwa msaada wa wa
hao. Watu wangu wanapenda mambo ya hivyo, lakini mwisho kitatokea nini?

# 6

1 Tafuteni mahali salama, enyi watu wa Benjamini, kwa kuondoka Yerusalemu.
Pigeni tarumbeta zaTekoa. Simamisheni ishara juu ya Beth- Hakeremu, kwa uovu
unaonekana ukitokea kaskazinni; pigo kubwa linakuja. 2 Binti za Sayuni, warembo na
mwororo, wataangamizwa. 3 Wachungaji na kondoo wao watawaendea; wataweka
hema zao zikiwazunguka pande zote; kila mtu atachunga kwa mkono wake.
4 Jitakaseni wenyewe kwa miungu kwa ajili ya vita. Twendeni tukamvamie wakati wa
adhuhuri. Ni vibaya sana kwamba mchana unatoweka na vivuli vya jioni vinakuja.
5 Lakini tumvamieni usiku na na tuharibu ngome zake. 6 Kwa kuwa BWANA wa
majeshi asema hivi: Kateni miti yake, na tengenezeni vifusi vya kuitekea Yerualemu.
Huu ndio mji sahihi kuuteka, Kwa sababu umejaa ukandamizaji. 7 Kama vile kisima
kitoavyo maji, vivyo hivyo mji huu uzaavyo uovu. Uaribifu na jeuri vimesikika

kwake. Mateso na tauni viko mbele yangu daima. 8 Uadhibiswhe, ee Yerusalemu,
vingenevyo nitaondoka kwako na kukufanya ukiwa, na nchi isiyokaliwa na watu.
9 BWANA wa majeshi asema hivi, “Hakika wataokota mabaki ya Isreli waliobaki kama
zabibu. Nyosha mkono wako ili uchume zabibu. 10 Nitamwambia nani na kumwonya
nani ili wasikilize? Tazama! Masikio yao hayakutahariwa; hayawezi kutilia manani!
Tazama! Neno la BWANA limekuja kuwarudi, lakini hawalitaki.” 11 Lakini nimejazwa
na hasira za BWANA. Nimechoka kuizuia. Aliniambia, “Imwage mbele ya watoto
mitaani na katika makundi ya vijana. Kwa kuwa kila mume atachukuliwa pamoja
na mke wake; na kila mzee mwenye miaka mingi. 12 Nyumba zao watapewa watu
wengine, kwa kuwa nitawavamia wakazi wa nchi kwa mkono wangu - asema BWANA
wa majeshi. 13 BWANA amesema hayo kutoka kwa mdogo hadi kwa mkubwa, kila
mmoja anatamani mapato ya udanganyifu. Kuanzia kuhani hadi nabii, Kila mmoja
anafanya hila. 14 Lakini wameponya vidonda vya watu wangu kwa juu juu tu.
Wanasema, 'Amani! Amani! na kumbe amani haipo. 15 Je, waliona aibu walipofanya
machukizo? Hasha, hawakuona aibu! Hawakuwa na aibu. Kwa hiyo wataanguka
pamoj na wale watakaoanguka wakati nitakpowaadhibu. Wataangushwa chini,”
asema BWANA. 16 BWANA asema hivi, `Simama kwenye njia panda utazame; uliza
nzile njia za zamani, 'Je, hii tabia njema iko wapi?' Kisha endelea nayo na tafuta
mahali pa kupumzika. Lakini watu wanasema, 'Hatutaenda.' 17 Niliweka walinzi
juu yenu ili wasikilize tarumbeta. Lakini walisema, 'Hatutasikiliza.' 18 Kwa hiyo,
sikilizeni, enyi mataifa! Tazameni, enyi mashahidi, muone kile kitakachowapata.
19 Sikia, wewe dunia! Tazama, niko tayari kuleta janga kwa watu hawa - matunda
ya fikra zao. Hawakusikiliza neno langu wala sheria zangu, badala yake walizikataa.
20 Huu ubani kutoka sheba unaopanda una maana gani kwangu? Au huu uudi kutoka
nchi ya mbali? Sadaka zenu za kuteketezwa hazikubaliki kwangu wala dhabihu
zenu. 21 Kwa hiyo BWANA asema hivi, 'Tazama, 'Niko tayari kuweka kikwazo dhidi
ya watu hawa. Watajikwaa juu yake - baba na watoto wao kwa pamoja watajikwaa.
Wakazi na jirani zao pia watapotea.' 22 BWANA asema hivi, 'Tazama watu wanakuja
toka nchi ya kaskazini. Kwa kuwa taifa kubwa limechochewa kutoka nchi ya mbali.
23 Watachukua pinde na mishale yao. Ni wakatili na hawana huruma. Sauti yao
ni kama muungurumo wa bahari, na wapanda farasi katika mfumo wa wanaume
wa vita, enyi binti wa Sayuni,”' 24 Tumesikia habai zao. Mikono yetu inalegea
kwa dhiki. Na maumivu yametukamata kama utungu wa mwanamke anayezaa.
25 Usiende nje mashambani, na usitembee barabarani, kwa kuwa upanga wa adui
na hofu vimekaribia. 26 Binti za watu wangu, jivikeni magunia na kugaagaa kwenye
majivu ya maombolezo ya mwana pekee. Ombolezeni kwa huzuni kuu, kwa kuwa
anayewaangamiza anakuja kwetu ghafula juu yetu. 27 “Nimekufanya wewe, Yeremia,
kuwajaribu watu wangu kama mtu anayepima fedha, kwa hiyo utachunguza na
kupima njia zao. 28 Wao ni watu wasumbufu miongoni mwa watu, wanaoenda huko
na kule wakisingizia wengine. Wote ni shaba na chuma, wakitenda kwa dhuluma.
29 Mifuo inafukuta kwa moto unaoziunguza; risasi inaunguzwa na moto. Risasi
tu ndiyo inayotoka kati yake, lakini haifai kitu kwa sababu uovu haujaondolewa.
30 Wataitwa taka za fedha, kwa sababu BWANA amewakataa.

# 7

1 Hili ndilo neno la BWANA lililomjia Yermia, 2 Simama katika lango la nyumba
ya BWANA na utangaze ujumbe huu! Sikiilizeni neno la BWANA, ninyi nyote watu
wa Yuda, ninyi mnaoingia katika malango haya kumwabudu BWANA. 3 BWANA wsa
majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: Tengenezeni njia zenu na kufanya mema,
nami nitawaacha muishi hapa. 4 Msitumainie maneno ya uongo mkisema, “Hekalu

la BWANA!, Hekalu la BWANA! Hekalu la BWANA!” [5] Bali kama mtazitengeneza njia
zenu na kufanya mema, kama mtatoa hukumu ya haki kati ya mtu na jirani yake
[6] -kama hamtanyonya anayekaa katika nchi, yatima, mjane, na kama hamtamwaga
damu ya mtu asiye na hatia mahali hapa, na kama hataenda kwa miungu mingine
kwa ajili ya maumivu yenu [7] -ndipo nitakapowaacha mkae mahali hapa, katika nchi
ambayo niliwapia mababu zenu toka zamani na hata milele. [8] Tazama! Mnatumainia
maneno ya uongo ambayo hayawasaidii. [9] Je, mnaiba. mnaua, manafanya uzinzi? na
mnaapa kwa uongo na kufukiza uvumba kwa Baali na kwenda kwa miungu mingine
ambao hamkuwajua? [10] Je, mnakuja na kusimama mbele yangu katika nyumba
hii ambapo jina langu linatangazwa na kusema, “Tumeokoka.” hivyo mnaweza
kufanya machukizo yote haya? [11] Je, hii ndiyo nyumba inayobeba jina langu, pango
la wanyang'anyi mbele ya macho yenu? Lakini tazama, Nimeiona - BWANA asema.'
[12] Kwa hiyo uende mahali pangu kule Shiloh, Kule ambako mwanzoni niliruhusu
jina langu kukaa, na tazama kile nilichofanya pale kwa sababu ya maovu ya watu
wangu Israeli. [13] Kwa hiyo sasa, kwa sababu ya matendo yako haya yote - asema
BWANA - Nilikuambia mara kadhaa, lakini hukusikiliza. Nilikuita, lakini hukuitika.
[14] Kwa hiyo kile nilichofanya Shilo, ndicho ambacho pia nitakachofanya kwa nyumba
yangu hii inayoitwa kwa jina langu, nyumba amabyo ninyi mmeitumainia, mahali
hapa ambapo niliwapa ninyi na mababu zenu. [15] Kwa kuwa nitawafukuza mtoke
kwangu kama vile nilivyowafukuza ndugu zenu wote, uzao wote wa Efraimu.'
[16] Na wewe, Yeremia, usiwaombee watu hawa, na usiinue maombolezo ya kilio au
kuomba sala kwa niaba yao, na usinishi, kwa kuwa sitakusikiliza. [17] Kwani huoni
kile wanachofanya katika miji ya Yuda na katika mitaa ya Yerusalemu? [18] Watoto
wanakusanya kuni na baba zao huwasha moto! Wanawake hukanda unga ili kuoka
mikate kwa ajili ya malikia wa mbinguni na kumimina sadaka ya vinywaji kwa
miungu mingine ili kunikasirisha mimi. [19] Ni kweli wananikasirisha mimi? - asema
BWANA - Je, si wao wanaojikasirisha, ili kwamba aibu iwe juu yao? [20] Kwa hiyo
BWANA, Mungu asema hivi, 'Tazama, hasira na ghahdabu yangu zitamwagwa juu
ya mahali hapa, kwa watu wote na wanyama, juu ya miti katika mashamba na
mazao ya ardhi, Itawaka nayo haitazimishwa. [21] BWANA wa majeshi, Mungu wa
Israeli asema hivi, Jiongezeeni sadaka za kuteketezwa katika dhabihu zenu na nyama
zake. [22] Kwani wakati nilipowatoa mababu zenu kutoka nchi ya Misri, Sikuhitaji
chochote kutoka kwao. Sikuwapa amri juu ya maswala ya sadaka za kuteketezwa na
dhabihu. [23] Niliwapa amri hii tu, “Sikilizeni sauti yangu, nami nitakuwa Mungu wenu
nanyi mtakuwa watu wangu. Kwa hiyo muishi katika njia ambazo ninawaamuru,
ili mambo yenu yawe mazuri.” [24] Lakini hawkunisikiliza wala kuzingatia. Walishi
kwa kufuata mipango yao ya uasi ya mioyo ya maovu, kwa hiyo walirudi nyuma
badala ya kuendelea mbele. [25] Tangu siku ambayo mababu zenu walitoka katika
nchi ya Misri mpaka leo, Nimetuma watumishi wangu, manabii wangu, kwenu.
Niliendelea kuwatuma. [26] Lakini hawakuwasikiliza. Hawakuzingatia. Badala yake
walishupaza shingo zao. Walikuwa waovu zaidi ya mababu zao. [27] Kwa hiyo
yatangaze maneno haya yote kwao, japo hawatakusikiliza. Yatangaze mambo haya
kwao, lakini hawatakujibu. [28] Waambie kuwa hili ni taifa ambalo haliisikilizi sauti ya
BWANA, Mungu wake na lisilopokea mafundisho. Ukweli uneharibiwa na kukatwa
kutoka kwenye vinywa vyao. [29] Zikate nywele zako na kujinyoa, na kuzitupa. Imba
wimbo wa maombolezo katika maeneo yaliyo wazi. Kwa kuwa BWANA amekikataa
na kukitupa kizazi hiki cha hasira yake. [30] Kwa kuwa wana wa Yuda wamefanya
maovu mbele ya macho yangu - asema BWANA - wameweka machukizo yao katika
nyumba ambayo jina langu hunenwa, ili kulinajisi. [31] Kisha wamejenga mahali
palipoinuka pa Tofethi ambapo pako kwenye bonde la Ben Hinomu. Walifanya hivi

ili kuwachoma wana na binti zao kwenye moto - kitu ambacho mimi sikuamuru,
wala kuweka jambo hilo katika akili zangu. 32 Kwa hiyo, tazama siku zinakuja -
asema BWANA - ambapo hapataitwa tena Tofethi au bonde la Ben Hinomu. Litakuwa
bonde la machinjio; watazika maiti hapo Tofethi mpaka eneo lote lienee. 33 Mizoga
ya watu hawa itakuwa chakula cha ndege wa angani na wanyama wa duniani, na
hakutakuwa na mtu wa kuwafukuza. 34 Nitazikomesha katika miji ya Yuda na mitaa
ya Yerusalaemu sauti za kuiniuliwa na vicheko, Sauti ya bwana arusi na ya bibi arusi;
kwa kuwa nchi hiyo itakuwa ukiwa."

# 8

1 Wakati huo - BWANA asema - wataleta kutoka makaburini mifupa ya wafalme wa
Yuda na wakuu wake, mifupa ya makuhani na ya manabii na mifupa ya wakazi wa
Yerusalemu. 2 Kisha wataitandaza nje mchana kweupe na mbalamwezi na nyota zote
za angani; hivi vitu katika anga vimenifuata na kunitumikia, na kwamba vimetembea
na kutafuta, na kwamba vimeniabudu. Mifupa haitakusanywa na kuzikwa tena.
Itakuwa kama mavi juu ya uso wa dunia. 3 Na katika kila eneo lililobaki ambalo
nimewafukuza, Watachagua mauti badala ya uzima kwa ajili yao, wote ambao
watasalia kutokana na taifa hili ovu - asema BWANA wa majeshi. 4 Kwa hiyo
uwaambie, 'BWANA asema hivi: Je, kuna mtu anyeanguka na hasimami? Je, kuna
mtu anayepotea na hawezi kujaribu kurudi? 5 Kwa nini hawa watu, Yerusalemu,
wamegeukia uasi daima? Wanashikilia uongo na wanakataa kutubu. 6 Nilikaa kwa
uangalifu na nikasikiliza, lakini hawakuongea kilicho sahihi; hakuna aliyetubia uovu
wake, hakuna asemaye, "Nimefanya nini?" Kila mmoja wao huenda kule anakotaka,
kama farasi aendaye kasi vitani. 7 Hata koikoi angani hujua wakati sahihi; na njiwa,
na mbayuayu, n a korongo. Huhama kwa wakati sahihi, lakini watu wangu hawayajui
maagizo ya BWANA. 8 Kwa nini mnasema, "Sisi tuna hekima! na sheria ya BWANA
tunayoi?" Hakika, Tazama! Kalamu yenye uongo ya mwandishi imefanya uongo.
9 Wenye hekima wataaibishwa. Wameyeyuka na na kunaswa. Tazama! wanakataa
neno la BWANA, kwa hiyo hekima yao ni kwa ajili ya matumizi gani? 10 Kwa wake
zao nitawapa wengine, na mashamba yao kwa wale watakaowamiliki, kwa kuwa
kuanzia kijana hadi mkuu, kwa pamoja ni wachoyo! Kuanzia nabii hadi kuhani,
wote wanasema uongo. 11 Kwa kuwa wametibu jeraha ya binti za watu wangu
kwa juu juu. Walijisemea, "Amani, Amani," na kumbe hapakuwa na amani. 12 Je,
waliona aibu walipofanya machukizo? Hawakuaibika. Hawakuwa na utu. Kwa hiyo
wataanguka wakati wa adhabu, pamoja na wale walioanguka. Watatupwa chini,
asema BWANA. 13 Nitawaondoa kabisa - asema BWANA - hapatakuwa na zabibu
kwenye mizabibu yao, wala tini katika mitini yao. kwa kuwa jani litanyauka, na kile
nilichowapatia kitaisha. 14 Kwa nini tunakaa hapa? Njoni pamoja; twendeni kwenye
hiyo miji yenye maboma, na tutakaa kimya kule katika kifo. Kwa kuwa BWANA,
Mungu wetu atatunyamazisha. Atatufanya tunywe sumu, kwa kuwa tumemtenda
dhambi. 15 Tunatumainia amani, lakini hakutakuwa na jema. Tunatumainia wakati
wa uponyaji, lakini tazama kutakuwa na hofu. 16 Mkoromo wa farasi wake umesikika
kutoka Dani. Dunia nzima inatikisika kwa sababu ya sauti ya kukaribia kwa farasi
wake wenye nguvu. Kwa kuwa watakuja kuiangamiza nchi na utajiri wake, mji na
wote wakaao nadani yake. 17 Hebu tazama, ninawatuma nyoka kati yenu, fira ambao
hawawezi kuzuiliwa kwa uganga. Watawauma - asema BWANA,." 18 Huzuni yangu
haina ukomo, na moyo wangu unaugua. 19 Tazama! sauti ya maumivu ya binti wa
watu wangu kutoka mbali! Je, BWANA hayumo Sayuni? Je, mfalme wake hayumo
ndani yake? Kwa nini sasa wananichukiza kwa vitu vya kuchongwa na sanamu
za kigeni zilizo batili? 20 Mavuno yamepita, wakati wa hari umekwisha. Lakini

sisi hatujaokoka. 21 Nimeumia kwa sababu ya maumivu ya binti wa watu wangu.
Ninaomboleza kwa sababu ya mambo ya kushangaza ambayo yametokea kwake;
Nimeyeyuka. 22 Je, kule Gileadi hakuan dawa? Je, huko hayuko mponyaji? Kwa nini
uponyaji wa binti wa watu wangu hautokei?

# 9

1 Kama kichwa changu kingetoa maji, na macho yangu kuwa chemichemi ya
machozi! kwa kuwa natamani kulia usiku na mchana kwa ajili yao waliokuwa binti
za watu wangu ambao wameuawa. 2 Kama mtu anganipatia mahali pa wasafiri
nyikani ili nikae, mahali ambapo ningeenda kuwatelekeza watu wangu. Kama
ningewaacha, kwa kuwa wote ni wazinzi, kundi la wenye hiana! 3 asema BWANA,
“Huupinda ulimi wao kana kwamba ni upinde ili wapate kuongea uongo, lakini
si kwa uamiinifu wao kwamba wanapata nguvu duniani. Wanatoka uovu mmoja
hadi mwiingine. Hawanijui mimi.” 4 Kila mmoja wenu, awe mlinzi wa jirani yake
na usimwamini hata ndugu yako yeyote. kwa kuwa kila ndugu ni mwongo, 5 kila
jirani anatembea akilaghai. Kila mwanamume anakejeli jirani yake na haongei
ukweli. Ndimi zao hufundisha vitu vya uongo. Hujidhofisha ili kusema uongo.
6 Makazi yenu yako kati ya udanganyifu; kwa uongo wao wanakataa kunitambua
mimi. Asema BWANA.” 7 Kwa hiyo BWANA wa majeshi asema hivi, “Tazama, Niko
tayari kuwajaribu. Nitawajaribu nione. Jinsi gani niwezavyo kufanya kwa binti
za watu wangu? 8 Ndimi zao ni mishale iliyochongoka; huongea vitu vya uasi.
Kwa midomo yao wanatangaza amani pamoja na jirani zao, lakini katika mioyo
yao wanadanganya wakati wa kusubri. 9 Kwa nini nisiwaadhibu kwa sababu ya
mambo haya - asema BWANA na kwa nini nisijilipizie kisasi kwa taifa ambalo liko
kama hili? 10 Nitaimba wimbo wa kuomboleza na kulia kwa ajili ya milima, na
wimbo wa mazishi utaimbwa nyikani. Kwa kuwa wameteketezwa kwa hiyo hakuna
anAyeweza kupita kati kati yao. Hawatasikia sauti ya ng'ombe yeyote. Ndege
wa angani na wanyama wote wamekimbia. 11 Kwa hiyo nitaigeuza Yerusalemu
kuwa vifusi vya ukiwa, maficho ya mbweha. Nitaifanya miji ya Yuda kuwa miji
iliyoharibiwa isiyokaliwa na watu. 12 Ni nani mwenye hekima anayeyaelewa haya?
Je, kinywa cha BWANA kinatangaza nini kwake ili aweze kuyasema? Kwa nini
nchi imepotea? Imeharibiwa kama jangwa, ambapo hakuna apitaye kati kati yake.
13 BWANA asema, “Ni kwa sababu wameziacha sheria zake ambazo niliwatengenezea,
kwa sababu hawaisikilizi sauti yangu au kuishi kwa kuifuta. 14 Ni kwa sababu
wameishi kwa ushupavu wa mioyo yao na wamewafuata Mabaali kama baba zao
walivyowafundisha kufanya. 15 Kwa hiyo BWANA wa majeshi, Mungu wa Israeli,
asema hivi, 'Tazama, Ninataka kuwafanya hawa watu wale pakanga na kunywa
maji ya sumu. 16 Ndipo nitakapowasambaza kati ya mataifa ambayo hawajayajua,
wao wala mababu zao. Nitatuma upanga kwa ajili yao mpaka nimewaangamiza
wote kabisa.'” 17 BWANA wa majeshi asema hivi, “Yafikirini haya: Waiteni waliaji;
waje. Tumeni wanawake wenye taaluma ya kuomboleza, waje. 18 Waje haraka
waimbe wimbo wa maombolezo juu yetu, ili macho yetu yatokwe na machozi
na kope zetu zibubujikwe na maji. 19 Kwa kuwa sauti ya kilio imesikika Sayuni,
'Jinsi tulivyoharibiwa. Tumeaibishwa sana, kwa kuwa tumeitelekeza nchi tangu
walIpoangusha nyumba zetu.' 20 Kwa hiyo ninyi wanawake, sikieni neno la BWANA;
zingatieni ujumbe unaokuja toka kinywani mwake. Kisha wafundisheni binti zenu
wimbo wa maombolezo, na kila mwanamke wa jirani wimbo wa kilio. 21 Kwa
kuwa vifo vimekuja kupitia dirishani; vinaelekea mahali petu. Vinawaharibu watoto
kutoka nje na vijana kwenye viwanja vya miji. 22 Uyatangaze haya, 'Asema BWANA
- mizoga ya wanaume itaanguka kama mavi kwenye mashamba na kama mabua

baada ya mvunaji, na hapatakuwa na mtu wa kuyakusanya.'" 23 BWANA asema hivi,
"Usimwache mtu mwenye busara ajivune kwa ajili ya hekima yake, au shujaa kwa
sababu ya uwezo wake. Usimwache mtu tajiri ajivunie utajiri wake. 24 Kwa kuwa
kama mtu atajivunia chochote kile, acha iwe hivi, yeye awe na busra na kunijua
mimi. Kwa kuwa mimi ni BWANA, atendaye katika agano la wema, haki, na hukumu
duniani. Ni katika hili kwamba ninafurahia- asema BWANA. 25 Tazama, siku zaja -
asema BWANA wakati nitakapowaadhibu wote ambao hawajatahiriwa ambao wako
hivyo hivyo katika miili yao. 26 Nitaiadhibu Misri na Yuda, Edomu, watu wa Amoni,
Moabu, na watu wote wanaonyoa denge. Kwani mataifa yote haya hayajatahiriwa,
na nyumba yote ya Israeli ina moyo ambao haujatahiriwa."

# 10

1 "Sikilizeni neno ambalo BWANA anawaambieni, enyi nyumba ya Israeli. 2 BWANA
asema hivi, 'msijifunze njia za mataifa, na msishangazwe na ishara za mbinguni, kwa
kuwa mataifa hushangazwa na haya. 3 Kwa kuwa desturi za watu ni ubatili. Kwa
kuwa mtu mmoja hukata mti msituni; kazi ya mikono ya mtu na shoka. 4 Kisha
huzipamba kwa fedha na dhahabu. Huikaza kwa misumari na nyundo ili isitikisike.
5 Sanamu hizi ni mfano wa sanamu za kutishia ndege katika shamba la matango, kwa
kuwa haziwezi kusema chochote. Hubebwa, kwa kuwa haziwezi hata kusogea hatua
moja. Usiwaogope, Kwani hawawezi kutenda maovu wala mema." 6 Hakuna aliye
kama wewe, BWANA. Wewe ni mkuu, na jina lako lina nguvu. 7 Ni nani asiyekuwa
na hofu juu yako, wafalme wa mataifa? Kwa kuwa hiki ndicho unachostahili, kwa
kuwa hakuna wa kuwa kama wewe kati ya wote wenye hekima katika mataifa yote
au katika hali yao ya enzi. 8 Wote wako sawa, ni kama wanyama na wapumbavu,
wanafunzi wa samamu ambazo si chochote isipokuwa miti tu. 9 Wanaleta fedha
iliyofuliwa kutoka Tarshishi, na dhahabu kutoka Ufazi iliyotengenezwa na sonara,
ni kazi ya ustadi. Mavazi yao ni ya rangi ya samawi na urujuani. Watu wao stadi
waliyafanya haya yote. 10 Lakini BWANA ni Mungu wa kweli. Yeye ni Mungu aliye
hai na mfalme wa milele. Matetemeko yako katika hasira yake, na mataifa hayawezi
kuvumilia hasira yake. 11 Utawaambia hivi, "Miungu ambayo haikuumba mbingu
na nchi itaangamia katika dunia hii na chini ya mbingu." 12 Aliyeiumba dunia
kwa nguvu zake aliumba nchi kavu kwa hekima zake na kuzitandaza mbingu kwa
fahamu zake. 13 Sauti yake ndiyo itengenezayo muungurumo wa maji mbinguni,
naye huzileta mbingu katika mwisho wa dunia. Hutengeneza radi kwa ajili ya mvua
na kutuma upepo kutoka katika hazina yake. 14 Kila mtu amekuwa mjinga, hawana
maarifa. Kila mfua chuma ameaibishwa kwa sanamu zake. Maana sanamu yake
ya kuyeyushwa ni uongo; hakuna pumzi ndani yake. 15 Ni ubatili tu, ni kazi ya
udanganyifu; zitapotea wakati wa hukumu. 16 Lakini Mungu ni fungu la Yakobo,
si kama hawa, kwa kuwa yeye ndiye aliyeviumba vitu vyote. Israeli ni kabila
ya urithi wake; BWANA wa majeshi ndiye jina lake. 17 Kusanya vitu vyako na
uiache nchi, wewe ambaye umekuwa ukiishi katika mazingiwa haya. 18 Kwa kuwa
BWANA asema hivi, "Tazama, Ni tayari kuwatupa wakazi wa nchi nje wakati huu.
Nitawasababishia huzuni, na itakuwa hivyo." 19 Ole wangu! Kwa sababu ya mifupa
yangu iliyovunjika, Jeraha zangu zimeumia. Kwa hiyo nilisema. "Hakika haya ni
maumivu, lakini lazima nivumilie." 20 Hema yangu imeharibiwa, na kamba za hema
yangu zote zimekatwa. Wamewachukua watoto wangu wote, Kwa hiyo hawaishi
tena. Hakuna tena mtu wa kuitandaza hema yangu au wa kuziinua pazia za hema
yangu. 21 Kwa kuwa wachungaji wamekuwa wapumbavu. Hawamtafuti BWANA.
Kwa hiyo hawana mafanikio; Kondoo wao wote wamesambaa. 22 Taarifa imewadia,
"Tazama! inakuja, tetemeko kubwa linakuja kutoka katika nchi ya kaskazini kuifanya

miji ya Yuda kuwa ukiwa, na maficho ya mbweha. 23 Ninajua, BWANA, kwamba
njia ya mtu haiji kutoka kwake. Wala hakuna mtu atembeaye anayeongoza hatua
zake mwenyewe. 24 Ee BWANA, unirudi, kwa hukumu za haki, si kwa hasira zako
vinginevyo utaniangamiza. 25 Mwaga hasira zako kwa mataifa ambao hawakujui
na katika familia ambazo hawakuiti kwa jina lako. Kwa kuwa wamemla Yakobo na
kumwangamiza kabisa na kuyafanya makao yake kuwa ukiwa.

# 11

1 Hili ndilo neno lililojia Yeremia kutoka kwa Bwana, akasema, 2 “Sikiliza maneno
ya agano hili, uwaambie kila mtu wa Yuda na wenyeji wa Yerusalemu. 3 Uwaambie,
'Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi: na alaaniwe yeyote asiyesikiliza maneno ya
agano hili. 4 Hili ndilo agano nililowaamuru baba zenu walishike siku nilipowatoa
kutoka katika nchi ya Misri, kutoka tanuru ya chuma. Nikawaambia, “Sikilizeni
sauti yangu na mfanye mambo yote kama nilivyowaamuru, kwa kuwa mtakuwa
watu wangu nami nitakuwa Mungu wenu.” 5 Nisikilizeni ili nipate kukitimiza
kiapo nilichoapa kwa baba zenu, kiapo kwamba nitawapa nchi iliyojaa maziwa na
asali kama ilivyo leo.'” Kisha mimi Yeremia nikajibu na kusema, “Ndio, Bwana!”
6 Bwana akaniambia, “Hubiri habari hizi yote katika miji ya Yuda, na katika njia
za Yerusalemu. Sema, “Sikilizeni maneno ya agano hili na mkayafanye. 7 Kwa
maana nimewaagiza wazee wenu tangu siku ile niliyowaleta kutoka nchi ya Misri
hadi wakati huu wa sasa, nimewaonya mara kwa mara na kusema, “Sikilizeni sauti
yangu.'” 8 Lakini hawakusikiliza au wala kutega masikio yao. Kila mtu amekuwa
akitembea katika ukaidi wa moyo wake mbaya. Kwa hiyo nilileta laana zote katika
agano hili nililoamuru kuja juu yao. Lakini watu bado hawakuitii.” 9 Kisha Bwana
akaniambia, “Njama imeonekana kati ya watu wa Yuda na wenyeji wa Yerusalemu.
10 Wameugeukia uovu wa mababu zao wa mwanzo, ambao walikataa kusikiliza neno
langu, ambao badala yake walifuata miungu mingine ili kuabudu. Waisraeli na
nyumba ya Yuda walivunja agano langu nililoweka na baba zao. 11 Kwa hiyo Bwana
asema hivi, 'Tazameni, nitawaletea majanga juu yao, majanga ambayo hawataweza
kuyaepuka. Ndipo wataniita, lakini sitawasikiliza. 12 Miji ya Yuda na wenyeji wa
Yerusalemu watakwenda na kuiita miungu ambayo walitoa sadaka, lakini hakika
hawatawaokoa wakati wa majanga yao. 13 Kwa kuwa idadi ya miungu yako ewe
Yuda imeongezeka sawa na idadi ya miji yako. Na umefanya idadi ya madhabahu
ya aibu huko Yerusalemu, madhabahu ya kufukiza uvumba kwa Baali, sawa na
idadi ya njia zake. 14 Kwa hiyo wewe mwenyewe, Yeremia, usiwaombee watu
hawa. Lazima usiomboleze au kuomba kwa niaba yao. Kwa maana siwezi kusikiliza
wakati wananiita katika majanga yao. 15 Mpendwa wangu anafanya nini nyumbani
kwangu, ikiwa amekuwa na nia mbaya? Nyama za sadaka yako hazitakusaidia.
Unafurahi kwa sababu ya matendo yako mabaya. 16 Katika siku za nyuma Bwana
alikuita mti wa mzeituni wenye majani, mzuri wenye matunda mazuri. Lakini
atawasha moto juu yake ambayo itaonekana kama sauti ya dhoruba; matawi yake
yatavunjika. 17 Kwa maana Bwana wa majeshi, aliyekua amekusudia maafa juu yako,
kwa sababu ya matendo mabaya ambayo nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda
wamefanya-wamenikasirisha kwa kumtolea Baali sadaka.'” 18 Bwana alinijulisha
mambo haya, kwa hiyo nakayajua. Wewe, Bwana, umenifanya nione matendo
yao. 19 Nilikuwa kama kondoo mpole unayeongozwa na mchinjaji. Sikujua kwamba
walikuwa wameunda mipango dhidi yangu, “Hebu tuangamize mti na matunda yake!
Hebu tumkatilie mbali na nchi ya walio hai ili jina lake lisikumbukwe tena. 20 Lakini
Bwana wa majeshi ndiye mwamuzi mwenye haki ambaye huchunguza moyo na akili.
Mimi nitashuhudia kisasi chako dhidi yao, kwa kuwa nimekuletea kesi yangu kwako.

[21] Kwa hiyo Bwana asema hivi juu ya watu wa Anathothi, wanaotafuta uhai wako,
“wanasema, 'Usifanye unabii kwa jina la Bwana, usije utakufa kwa mkono wetu.'
[22] Kwa hiyo Bwana wa majeshi asema hivi, 'Tazameni, nitawaadhibu. Vijana wao
wenye nguvu watakufa kwa upanga. Wana wao na binti zao watakufa kwa njaa.
[23] Hakuna hata mmoja atakayeachwa, kwa maana nitaleta maafa dhidi ya watu wa
Anathothi, mwaka wa adhabu yao.'”

# 12

[1] Wewe ni mwenye haki, Bwana, wakati wowote ninapoleta mashitaka kwako.
Lazima nikuambie sababu yangu ya kulalamika: Kwa nini njia za waovu hufanikiwa?
Watu wote wasiokuwa na imani wanafanikiwa. [2] Wewe uliwapanda nao wakawa
na mizizi. Wanaendelea kuzaa matunda. Wewe upo karibu nao katika vinywa
vyao, lakini mbali na mioyo yao. [3] Lakini wewe mwenyewe unanijua, Bwana.
Umeona mimi na kuchunguza moyo wangu. Waondoe kama kondoo wa kuchinjwa.
Ukakaweke tayari kwa siku ya kuchinjwa. [4] Je! Nchi itakauka kwa muda gani, na
mimea katika kila shamba itaota kwa sababu ya uovu wa wenyeji wake? Wanyama
na ndege wameondolewa. Hakika, watu wanasema, “Mungu hajui nini kitatokea
kwetu.” [5] Bwana akasema, “Kweli, wewe, Yeremia, umetembea na askari wa miguu
na wamechoka, unawezaje kushindana dhidi ya farasi? Ikiwa unashuka chini ya
nchi iliyo salama, utafanyaje katika misitu karibu na Yordani? [6] Kwa maana hata
ndugu zako na familia ya baba yako wamekudharau na kukukemea kwa sauti
kubwa. Usiwaamini, hata kama wanasema mambo mazuri kwako. [7] Nimeiacha
nyumba yangu; Nimeacha urithi wangu. Nimewatia watu wangu wapendwa
mikononi mwa adui zake. [8] Urithi wangu umekuwa kwangu kama simba katika
tundu; yeye hujiweka juu yangu kwa sauti yake mwenyewe, hivyo nimemchukia.
[9] Malipo yangu ya thamani ni fisi, na ndege wenye madoadoa karibu na kichwa
chake. Nenda, ukakusanye viumbe vyote vilivyomo katika mashamba, na uwalete ili
wale. [10] Wachungaji wengi wameharibu shamba langu la mizabibu. Wameipoteza
sehemu yangu yote ya ardhi; Waligeuza sehemu yangu nzuri kuwa jangwa, ukiwa.
[11] Wamemfanya kuwa ukiwa. Ninaomboleza kwa ajili yake; yeye ni ukiwa. Nchi yote
imefanywa kuwa ukiwa, kwa maana hakuna mtu aliyeweka haya moyoni mwake.
[12] Waangamizi wamekuja juu ya maeneo yote yaliyo wazi jangwani, kwa maana
upanga wa Bwana unakula kutoka upande mmoja wa nchi hadi mwingine. Hakuna
usalama katika nchi kwa kiumbe chochote kilicho hai. [13] Walipanda ngano lakini
mavuno ya miiba. Wao wamechoka kutokana na kazi lakini hawajapata chochote.
Basi muaibike kwa faida yenu kwa sababu ya ghadhabu ya Bwana.” [14] Bwana
asema hivi dhidi ya majirani zangu wote, waovu wanaopiga milki niliyowarithisha
watu wangu Israeli, “Tazama, mimi ndimi ambaye nitawafukuza kutoka nchi yao
wenyewe, nami nitaifuta nyumba ya Yuda kutoka kati yao. [15] Ndipo baada ya
kuangamiza mataifa hayo, itatokea kwamba nitakuwa na huruma juu yao na
kuwaleta tena; Nitawarudi-kila mtu kwa urithi wake na nchi yake. [16] Kisha itakuwa
ikiwa mataifa hayo yatajifunza kwa makini njia za watu wangu, kuapa kwa jina langu
'Kama Bwana anaishivyo!' vile vile kama walivyowafundishwa watu wangu kuapa
kwa Baali, basi watajengwa katikati ya watu wangu. [17] Lakini kama hakuna yeyote
anayesikiliza, basi nitaling'oa taifa hilo. Kwa hakika litang'olewa na kuharibiwa-hili
ndilo tamko la Bwana.”

# 13

[1] Bwana aliniambia hivi, “Nenda ukape nguo ya kitani na kuiweka karibu na kiuno
chako, lakini usiiweke kwenye maji kwanza.” [2] Kwa hiyo nilinunua vazi kama vile

Bwana alivyoagiza, na nikafunga karibu na kiuno changu. 3 Ndipo neno la Bwana
likanijia mara ya pili, kusema, 4 “Twaa vazi lako ulilolinunua lililo karibu na kiuno
chako, uinuke, ukasafiri mpaka Frati. Ukaifiche huko katika mwamba wa jabali.
5 Basi nikaenda na kuificha katika Frati kama vile Bwana alivyoniamuru. 6 Baada ya
siku nyingi, Bwana akaniambia, “Simama, urudi Frati. Ukaichukue nguo ambayo
nilikuambia ufiche.” 7 Kwa hiyo nikarudi Frati na kuchimba na kuchukua nguo
mahali pale nilipoificha. Lakini tazama! Nguo hiyo ilikuwa imeharibika; haikuwa
nzuri kabisa. 8 Ndipo neno la Bwana likanijia tena, kusema, 9 “Bwana asema hivi,
Nitakiangamiza kiburi cha Yuda na Yerusalemu. 10 Watu hawa waovu wanaokataa
kusikia neno langu, ambao huenda katika ugumu wa mioyo yao, ambao hufuata
miungu mingine ili kuabudu na kuinama-watakuwa kama hii nguo isiyofaa kwa
lolote. 11 Kwa maana kama vile vazi lililofungwa kwenye viuno vya mtu, ndivyo
nimefainya nyumba yote ya Israeli na nyumba yote ya Yuda zimefungwa kwangu- hili
ndilo tamko la Bwana-wawe watu wangu, ili kunifanya jina, sifa, na heshima. Lakini
hawakunisikiliza. 12 Basi uwaambie neno hili, 'Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi
Kila chupa itajazwa divai.' Watakuambia, 'Je, hatujui kwamba kila chupa itajazwa
divai?' 13 Basi uwaambie,' Bwana asema hivi: Tazama, nitawajaza kila mkaaji wa
nchi hii ulevi, na wafalme wanaokaa kiti cha Daudi, na makuhani, na manabii, na
wenyeji wote wa Yerusalemu. 14 Ndipo nitawagonganisha kila mtu na mwenzake
baba na watoto wao pamoja; hili ndilo tamko la Bwana-sitawahurumia au kuwa
na huruma, wala sitawarehemu kutoka kwenye uharibifu. 15 Sikilizeni na makini.
Msiwe na kiburi, kwa kuwa Bwana amesema. 16 Mtukuze Bwana, Mungu wako, kabla
ya hajaleta giza, na kabla ya kuifanya miguu yako kuwa na mashaka juu ya milima
wakati wa jioni. Kwa maana unatarajia mwanga, lakini ataugeuza kuwa mahali pa
giza, na kuwa giza nene. 17 Kwa hiyo ikiwa husikilizi, nitaomboleza peke yangu
kwa sababu ya kiburi chako. Hakika macho yangu yatalia na kutoa machozi, kwa
sababu kundi la Bwana limechukuliwa mateka. 18 “Mwambieni mfalme na mama
wa malkia, 'Jinyenyekezeni, na kukaa chini, kwa maana taji juu ya kichwa chako,
kiburi chako na utukufu wako, umeanguka.' 19 Miji ya Negebu itafungwa, bila mtu
wa kufungua. Yuda watachukuliwa mateka, wote uhamishoni. 20 Inua macho yako na
angalia wale wanaokuja kutoka kaskazini. Je, ni kundi gani alilokupa, kundi ambalo
lilikuwa zuri sana kwako? 21 Je, unasema nini wakati Mungu anawaweka wale ambao
uliwafundisha kuwa marafiki? Je, huu si mwanzo wa maumivu ya utungu ambayo
yatakuchukua kama mwanamke aliye katika kuzaa? 22 Kisha unaweza kusema
moyoni mwako, 'Kwa nini mambo haya yanatokea kwangu?' Itakuwa kwa uovu wa
maovu yako ambapo marinda yako yamefunuliwa na umeumizwa. 23 Je, watu wa
Kushi hubadilisha rangi yao ya ngozi, au chui hubadilisha madoa yake? Ikiwa ndivyo,
basi wewe mwenyewe, ingawa unazoea uovu, utaweza kufanya mema. 24 Kwa
hiyo nitawaangamiza kama makapi ambayo yanaangamia katika upepo wa jangwa.
25 Hii ndiyo niliyokupa, sehemu ambayo nimekuagiza kwako-hili ndilo tamko la
Bwana - kwa sababu umenisahau na kuamini katika udanganyifu. 26 Kwa hiyo mimi
mwenyewe nitaondoa nguo zako, na sehemu zako za siri zitaonekana. 27 Uzinzi na
ubembe wako, aibu ya tabia yako ya uasherati kwenye milima na katika mashamba!
Nitayafanya yaonekane, mambo haya ya machukizo! Ole wako, Yerusalemu! Hutaki
kuwa safi. Je! Hili litaendelea kwa muda gani?”

# 14

1 Neno la Bwana lilimjia Yeremia kuhusu ukame, 2 “Wayahudi waomboleze; basi
milango yake ianguke. Wao wanaomboleza kwa ajili ya ardhi; Kilio chao kwa
Yerusalemu kimepaa juu. 3 Wenye nguvu huwatuma watumishi wao kwa ajili

ya maji. Wanapoingia kwenye visima, hawawezi kupata maji. Wote wanarudi
hawajafanikiwa; Wao hufunika vichwa vyao na aibu. [4] Kwa sababu hii ardhi
imepasuka, kwa maana hakuna mvua katika nchi. Wakulima huwa na aibu na
kufunika vichwa vyao. [5] Kwa maana hata kunguru huwaacha wanawe katika
mashamba, kwa maana hakuna nyasi. [6] Punda mwitu husimama kwenye mabonde
yaliyo wazi na hupiga upepo kama mbweha. Macho yao yanashindwa kufanya
kazi, kwa maana hakuna mimea. [7] Hata ingawa maovu yetu yanatushuhudia,
Bwana, tenda kwa ajili ya jina lako. Kwa sababu matendo yetu yasiyo na imani
yamezidi; tumekutenda dhambi. [8] Matumaini ya Israeli, yule anayemwokoa wakati
wa dhiki, kwa nini utakuwa kama mgeni katika nchi, kama mtu akaaye nchi ya
kigeni ambaye hujinyoosha na kutumia hutumia usiku mmoja tu? [9] Kwa nini
utakuwa kama mtu aliyechanganyikiwa, kama shujaa ambaye hawezi kuokoa mtu
yeyote? Kwa maana wewe u katikati yetu, Bwana! Jina lako limetangazwa juu
yetu. Usiondoke [10] Bwana awaambia hivi watu hawa “Kwa kuwa wanapenda
kutanga tanga, hawakuzuia miguu yao kufanya hivyo.” Bwana hafurahi nao. Sasa
anawakumbusha uovu wao na ameadhibu dhambi zao. [11] Bwana akaniambia,
Usiombe kwa ajili ya watu hawa. [12] Maana ikiwa wanafunga, sitasikiliza kulia kwao;
na wanapotoa sadaka za kuteketezwa na sadaka za unga, sitawafurahia. Kwa maana
nitawaangamiza kwa upanga, njaa, na tauni. [13] Ndipo nikasema, “Ee Bwana, Bwana!
Angalia! mabii wanawaambia watu, 'Huwezi kuona upanga; hakutakuwa na njaa
kwako, kwa kuwa nitakupa usalama wa kweli mahali hapa.'” [14] Bwana akaniambia,
'manabii wanatabiri uongo kwa jina langu. Sikuwafukuza, wala sikuwapa amri au
kusema nao. Lakini maono ya udanganyifu na ya maana, uchawi wa udanganyifu
unaotokana na akili zao ndicho wanachowahubiria.” [15] Kwa hiyo Bwana asema hivi,
“Kwa habari ya manabii wakihubiri kwa jina langu, ambao mimi siwakutuma; wale
wanaosema kuwa hakutakuwa na upanga wala njaa katika nchi hii mabii hawa
wataangamia kwa upanga na njaa. [16] Na watu waliopewa utabiri watafukuzwa
nje ya barabara za Yerusalemu kwa sababu ya njaa na upanga; kwa kuwa hakuna
mtu wa kuwazikas-wao, na wake zao, na wana wao, wala binti zao; kwa maana
nitamwaga uovu wao wenyewe juu yao. [17] Sema neno hili kwao 'Acha macho
yangu yatokwe machozi, usiku na mchana. wala yasikome, kwa kuwa kutakuwa
na kuanguka kwa bikira, binti ya watu wangu - jeraha kubwa lisilotibika. [18] Ikiwa
nitatoka kwenye shamba basi angalia! kuna wale waliouawa kwa upanga. Na kama
nitakuja mjini, basi, tazama! kuna wale walio na ugonjwa wa njaa. Hata nabii
na kuhani wote wanatembea juu ya nchi bila maarifa.'” [19] Je! Umemkataa kabisa
Yuda? Je, unaichukia Sayuni? Kwa nini umetupiga wakati hakuna uponyaji kwetu?
Tulitumaini amani, lakini hapakuwa na kitu kizuri-na kwa wakati wa uponyaji, lakini
tazama, kuna hofu tu. [20] Tunakubali, Bwana, makosa yetu, uovu wa babu zetu, kwa
kuwa tumekukosea. [21] Usitukatae! Kwa ajili ya jina lako, usikifedheheshe kiti chako
cha enzi cha utukufu. Kumbuka na usivunje agano lako na sisi. [22] Je, kuna miongoni
mwa sanamu za mataifa yeyote zinazoweza kuifanya mbingu kutoa mvua? Je, si
wewe, Bwana Mungu wetu, ambaye hufanya jambo hili? Tunatumaini kwako, kwa
kuwa umefanya mambo haya yote.

# 15

[1] Kisha Bwana akaniambia, “Hata kama Musa au Samweli walisimama mbele
yangu, bado sitawafikiria watu hawa. Watoe mbele yangu, ili waweze kuondoka.
[2] Ikiwa watakuambia, 'Tunapaswa kwenda wapi?' Kisha uwaambie, 'Bwana asema
hivi Wale wanaotakiwa kufa wanapaswa kufa; wale waliotayarishwa kwa upanga
wanapaswa kwenda kwa upanga. Wale waliopelekwa kwa njaa wanapaswa kwenda

kwa njaa; na wale waliopelekwa uhamisho wanapaswa kuhamishwa.' 3 Kwa
kuwa nitawapa kwa makundi manne-hili ndilo tamko la Bwana-upanga wa kuua
wengine, mbwa wararue, ndege wa angani na mnyama mkali wale na kuangamiza.
4 Nitawafanyia jambo lenye kutisha kwa falme zote za dunia, kwa sababu Manase
mwana wa Hezekia, mfalme wa Yuda, alifanya huko Yerusalemu. 5 Kwa maana
ni nani atakayewahurumia, Yerusalemu? Ni nani atakayeomboleza kwa ajili yako?
Nani atakayegeuka kuuliza kuhusu ustawi wako? 6 Umeniacha-hili ndilo tamko la
Bwana-umerudi nyuma. Kwa hiyo nitawapiga kwa mkono wangu na kukuangamiza.
Nimechoka kuwahurumia. 7 Kwa hiyo nitawapepea kwa kipepeo katika milango ya
nchi. Nitawafukuza. Nitawaangamiza watu wangu kwani hawakurudi na kuziacha
njia zao. 8 Nitawafanya wajane wao kuwa zaidi ya mchanga wa bahari. Dhidi
ya mama wa vijana nitamtuma mwangamizi mchana. Nitafanya mshtuko na hofu
ghafla kuanguka juu yao. 9 Mama aliyezaa watoto saba ataharibika. Atashuka.
Jua lake limekuchwa wakati bado ni siku. Yeye atakuwa na aibu na kufedheheka,
kwa kuwa nitawatoa wale waliosalia kwa upanga mbele ya maadui zao-hili ndilo
tamko la Bwana." 10 Ole wangu, mama yangu! Kwa maana umenizaa, mimi
ambaye ni mtu wa kushindana na hoja katika nchi yote. Sijakopesha, wala hakuna
mtu aliyenikopesha, lakini wote wananilaani. 11 Bwana akasema "Je sitakuokoa
kwa manufaa? Kwa hakika nitawafanya maadui wako waombe msaada wakati wa
msiba na dhiki. 12 Je, mtu anaweza kusaga chuma? Hasa chuma kutoka kaskazini
iliyochanganywa na shaba? 13 Nitawapa adui zako utajiri wako na hazina yako
kama nyara za bure. Nitafanya hili kwa sababu ya dhambi zako zote zilizofanywa
ndani ya mipaka yako yote. 14 Ndipo nitakufanya utumikie adui zako katika nchi
ambayo huijui, maana moto utawaka, ukawaka katika ghadhabu yangu juu yako."
15 Wewe mwenyewe wajua, Bwana! Unikumbuke na kunisaidia. Ukanilipie kisasi
kwa ajili ya wanaonifuata. Katika uvumilivu wako usiniondoe. Utambue kwamba
nimekuwa na aibu kwa ajili yako. Maneno yako yamepatikana, na nikayala.
16 Maneno yako yalikuwa furaha kwangu, furaha yangu kwa moyo wangu; kwa
maana jina lako linatangazwa juu yangu, Bwana, Mungu wa majeshi. 17 Sikuketi
katika mkutano wa wale waliosherehekea au waliofurahi. Nimeketi kwa faragha
kwa sababu ya mkono wako wenye nguvu, kwa maana umenijaza na hasira. 18 Kwa
nini maumivu yangu yanaendelea na jeraha langu halitibiki, linakataa kuponywa?
Je, utakuwa kama maji ya udanganyifu kwangu, maji yanayokauka? 19 Kwa hiyo
Bwana asema hivi, "Yeremia, Ikiwa utatubu, nitakurejesha, nawe utasimama mbele
yangu na kunitumikia. Kwa maana ukitenganisha mambo ya kipumbavu kwa vitu
vya thamani, utakuwa kama kinywa changu. Watu watakuja kwako, lakini wewe
mwenyewe usirudi kwao. 20 Nitakufanya kama ukuta wa shaba usioweza kuingilika
kwa watu hawa, nao watapigana vita dhidi yako. Lakini hawatakushinda, kwa
kuwa mimi ni pamoja nawe ili kuokoa na kukuponya-hili ndilo tamko la Bwana-
21 kwa maana nitakuokoa mikononi mwa waovu na kukukomboa katika mkono wa
mshindani."

## 16

1 Ndipo neno la Bwana likanijia, kusema, 2 "Usiwe na mke, wala usiwe na wana au
binti hapa. 3 Kwa kuwa Bwana asema hivi kwa wana na binti ambao wamezaliwa
hapa, kwa mama waliowabeba, na kwa baba waliowafanya wazaliwe katika nchi
hii, 4 'Watakufa vifo vya magonjwa. Hawataliliwa wala kuzikwa. Watakuwa kama
samadi juu ya nchi. Kwa maana wataangamizwa kwa upanga na njaa, na miili yao
itakuwa chakula cha ndege wa angani na wanyama wa dunia.' 5 Maana Bwana
asema hivi, 'Usiingie nyumba yoyote yenye kuomboleza. Usiende kuwaombolezea,

wala usihuzunike kwa ajili ya watu hawa. Kwa maana nimeondoa amani yangu,
uaminifu wa agano, na huruma, kutoka kwa watu hawa! Ndivyo asemavyo Bwana;
6 kwa hiyo wakuu na wadogo watakufa katika nchi hii. Wala hawatazikwa, wala
hakuna yeyote atakayeomboleza kwa ajili yao. Hakuna mtu atakayejikata-kata au
kunyoa vichwa vyao kwa ajili yao. 7 Hakuna mtu anayepaswa kugawa chakula
chochote wakati wa kuomboleza ili kuwafariji kwa sababu ya vifo, na hawatawapa
kikombe cha faraja kwa baba yake au mama yake ili kuwafariji. 8 Usiende kwenye
nyumba ya karamu ili ukae pamoja nao ili kula au kunywa. 9 Kwa maana Bwana
wa majeshi, Mungu wa Israeli, asema hivi, 'Tazama, mbele yako, siku zako na
mahali hapa, nitakomesha sauti ya furaha na sherehe, sauti ya bwana na bibi
arusi. ' 10 Kisha itatokea kwamba utawaambia watu hawa maneno haya yote, na
watakuambia, 'Mbona Bwana amesema maafa yote haya juu yetu? Uovu wetu ni
uovu gani na dhambi yetu tuliyomtendea Bwana, Mungu wetu?' 11 Basi uwaambie,
'hii ndiyo ahadi ya Bwana; Kwa sababu baba zenu waliniacha, nao wakafuata miungu
mingine, wakaiabudu na kuisujudia. Waliniacha na hawakuishika sheria yangu.
12 Lakini ninyi wenyewe mmeleta uovu zaidi kuliko baba zenu, kwa maana, kila
mtu anaenda kwa ukaidi wa moyo wake mbaya; hakuna mtu anayenisikiliza. 13 Kwa
hiyo nitawafukuza kutoka nchi hii mpaka nchi msiyoijua, wewe wala baba zako,
nanyi mtaiabudu miungu mingine huko mchana na usiku, kwa maana mimi sitawapa
fadhili zangu.' 14 Kwa hiyo tazama! Siku zinakuja-hili ndilo tamko la Bwana-ambapo
hawatasema tena, 'Kama Bwana aishivyo, yeye aliyewaleta wana wa Israeli kutoka
nchi ya Misri.' 15 Kwa maana, kama Bwana aishivyo, yeye aliyewaleta wana wa Israeli
kutoka nchi ya kaskazini, na kutoka nchi aliyowaangamiza, nitawarudisha katika
nchi niliyowapa baba zao. 16 Angalia! hili ni tamko la Bwana-Nitatuma wavuvi wengi-
kwa hiyo watawavua watu. Baada ya hayo nitatuma wawindaji wengi ili waweze
kuwinda kati ya milima na vilima vyote, na katika miamba ya mwamba. 17 Kwa kuwa
macho yangu yapo juu ya njia zao zote; hawawezi kujificha mbele yangu. Uovu wao
hauwezi kufichika mbele ya macho yangu. 18 Nami kwanza nitawalipa mara mbili
uovu na dhambi zao kwa kuwa wameichafua nchi yangu sanamu za machukizo, na
kwa kujaza urithi wangu na sanamu zao za machukizo. 19 Ee Bwana, wewe ndiwe
ngome yangu, na kimbilio langu, na mahali pa usalama wangu siku ya shida. Mataifa
yatakujia kwako kutoka mwisho wa dunia na kusema, 'Hakika baba zetu walirithi
udanganyifu. Ubatili mtupu; hakuna faida ndani yao. Je! 20 Watu hufanya miungu
kwa ajili yao wenyewe? Lakini wao sio miungu. 21 Kwa hiyo tazama! Nitawafanya
wajue wakati huu, nitawafanya watambue mkono wangu na nguvu zangu, kwa hiyo
watajua kwamba Yahweh ni jina langu.”

# 17

1 “Dhambi ya Yuda imeandikwa kwa kalamu ya chuma yenye ncha ya almasi.
Imechongwa kwenye kibao cha mioyo yao na kwenye pembe za madhabahu zako.
2 Watoto wao wanakumbuka madhabahu zao na miti yao ya Ashera kwa miti ya
majani kwenye milima mirefu. 3 Mlima wangu katika nchi ya wazi na mali yako
yote pamoja na hazina zako zote, nitakupa kama nyara kwa wengine. Hiyo ndiyo
thamani ya maeneo yako ya juu na dhambi iliyo katika maeneo yako yote. 4 Utapoteza
urithi niliokupa. Nitakutumikisha kwa adui zako katika nchi ambayo hujui, kwa
maana umewasha moto katika ghadhabu yangu, ambao utakawaka milele.” 5 Bwana
asema, “Mtu anayemtegemea mwanadamu amelaaniwa; amfanyaye mwanadamu
kuwa nguvu yake na kugeuza moyo wake mbali na Bwana. 6 Kwa maana atakuwa
kama msitu mdogo katika Araba na hawezi kuona kitu kizuri kikija. Atakaa katika
maeneo ya mawe jangwani, nchi isiyokuwa na wakazi. 7 Lakini mtu anayemtegemea

Bwana amebarikiwa, kwa kuwa Bwana ndiye tumaini lake. 8 Kwa maana atakuwa
kama mmea karibu na maji kando ya mto; mizizi yake itaenea. Hawezi kuona joto
likija, kwa kuwa majani yake yatakuwa mabichi. Kisha mwaka wa ukame hawezi
kuwa na wasiwasi, wala hataacha kuzalisha matunda. 9 Moyo ni mdanganyifu
zaidi kuliko kitu kingine chochote. Una mgonjwa; ni nani anayeweza kuelewa?
10 Mimi ni Bwana, ninayechunguza akili, ambaye hujaribu viuno. Ninampa kila
mtu kulingana na njia zake, kulingana na matunda ya matendo yake. 11 kama
Kware akusanyaye mayai asiyotaga. Mtu anaweza kuwa tajiri kwa udhalimu, lakini
wakati nusu ya siku zake ukipita, utajiri huo utamuacha, na mwishowe atakuwa
mpumbavu." 12 "Mahali pa hekalu letu ni kiti cha enzi cha utukufu, kilichoinuliwa
tangu mwanzo. 13 Bwana ni tumaini la Israeli. Wote ambao wanakuacha watakuwa
na aibu. Wale walio katika nchi ambao wanageuka kutoka kwako watauliwa. Kwa
maana wamwacha Bwana, chemchemi ya maji yaliyo hai. 14 Niponye, Bwana, na
mimi nitaponywa! Niokoe mimi, nami nitaokolewa. Kwa maana wewe ndio wimbo
wangu wa sifa. 15 Tazama, wananiambia, 'Neno la Bwana liko wapi? Hebu lije!'
16 Mimi sikuwahi kuacha kuwa mchungaji nyuma yako. Sikuitamani siku ya maafa.
Unajua yaliyotoka mdomoni mwangu. Yalifanyika mbele ya uwepo wako. 17 Usiwe
sababu ya hofu kwangu. Wewe ni kimbilio langu siku ya msiba. 18 Waaibike watu
wanaoniudhi, lakini nisiaibike mimi. Wataogopa, lakini usiache nifadhaike. Tuma
siku ya maafa dhidi yao na kuwaangamiza maradufu." 19 Bwana akaniambia hivi,:
"Nenda ukasimame katika lango la watu ambako wafalme wa Yuda wanaingia na
kutoka, basi katika malango mengine yote ya Yerusalemu. 20 Uwaambie, 'Sikieni neno
la Bwana, wafalme wa Yuda, na ninyi watu wote wa Yuda, na kila mtu wa Yerusalemu
atakayeingia kwa njia ya malango haya. 21 Bwana asema hivi: "Jihadharini kwa ajili
ya maisha yenu na msichukue mzigo siku ya sabato ili muilete katika malango ya
Yerusalemu. 22 Wala msilete mzigo nje ya nyumba zenu siku ya sabato. Msifanye kazi
yoyote, lakini muitenge siku ya Sabato, kama nilivyowaagiza wazee wako kufanya.'"
23 Hawakusikiliza wala kutaega masikio yao, lakini walifanya shingo zao kuwa ngumu
ili wasinisikilize wala kukubali maonyo. 24 Itatokea kwamba ikiwa mtanisikiliza
kweli-hili ndilo tamko la Bwana-na msilete mzigo kwenye malango ya jiji hili siku
ya sabato lakini badala yake mkatenga siku ya sabato kwa Bwana na msifanye kazi
yoyote juu yake - 25 basi wafalme, wakuu, na wale wanaokaa kiti cha Daudi wataingia
malango ya mji huu kwa magari na farasi, wao na viongozi wao, watu wa Yuda na
wenyeji wa Yerusalemu. Na mji huu utakaa milele. 26 Watakuja kutoka miji ya Yuda
na kutoka pande zote za Yerusalemu, kutoka nchi ya Benyamini na visiwa vya chini,
kutoka milimani na kutoka kaskazini, wakileta sadaka za kuteketezwa, dhabihu,
sadaka za nafaka na ubani, sadaka za shukrani kwenye nyumba ya Bwana. 27 Lakini
ikiwa hamtasikiliza-kutakasa siku ya Sabato, kutochukua mizigo nzito, wala msiingie
milango ya Yerusalemu siku ya sabato, nitawasha moto katika malango yake, nao
utaangamiza majumba kuteketeza ngome za Yerusalemu, na hauwezi kuzimika.

# 18

1 Neno la Bwana lilimjia Yeremia, kusema, 2 "Simama, uende kwa nyumba ya
mfinyanzi; kwa maana nitakusikilizisha neno langu huko. 3 Basi, nikaenda nyumbani
kwa mfinyanzi, na tazama! Mfinyanzi alikuwa akifanya kazi kwenye gurudumu la
mfinyanzi. 4 Lakini chombo cha udongo ambacho alikuwa akikifinyanga kiliharibika
mkononi mwake, kwa hiyo alibadili mawazo yake na akafanya kitu kingine ambacho
kilionekana kuwa kizuri machoni pake. 5 Ndipo neno la Bwana likanijia, kusema,
6 "Je, siwezi kuwa kama huyu mfinyanzi kwenu, nyumba ya Israeli? Angalia! Kama
udongo katika mkono wa mfinyanzi-ndivyo ulivyo mkononi mwangu, nyumba ya

Israeli. [7] Kwa wakati mmoja, ninaweza kutangaza jambo fulani juu ya taifa au
ufalme, kwamba nitaufukuza, kuuvunja, au kuuharibu. [8] Lakini kama taifa ambalo
nimefanya tamko hilo linageuka na kuacha maovu yake, basi nitaghairi nisitende
maafa niliyokuwa nimepanga. [9] Wakati mwingine, ninaweza kutangaza jambo fulani
kuhusu taifa au ufalme, kwamba nitaujenga au kuupanda. [10] Lakini ikiwa watafanya
mabaya machoni pangu kwa kutosikiliza sauti yangu, basi nitaghairi mema ambayo
nilikuwa nimewaambia nitawafanyia. [11] Basi sasa, waambie watu wa Yuda na
wenyeji wa Yerusalemu, ukisema, 'Bwana asema hivi: Tazameni, nitawaangamiza.
Mimi ni karibu kufinyanga mabaya dhidi yenu. Tubuni, kila mtu kutoka njia yake
mbaya, hivyo njia zako na matendo yako yatakuletea mema.' [12] Lakini watasema, 'Hili
halina maana. Tutafanya kulingana na mipango yetu wenyewe. Kila mmoja wetu
atafanya mabaya kwa kuufuata uchupavu wa moyo wake.' [13] Kwa hiyo Bwana asema
hivi, 'Uliza watu wa mataifa, ambao wamewahi kusikia habari kama hii? Bikira
wa Israeli amefanya kitendo cha kutisha. [14] Je, theluji ya Lebanoni imetoka milima
yenye miamba juu ya pande zake? Je, mito ya mlima inayotoka mbali iliharibiwa,
mito hiyo ya baridi? [15] Hata hivyo watu wangu wamesahau. Wamefanya sadaka
kwa sanamu zisizo na maana na wamefanya mashaka katika njia zao; wameacha
njia za kale za kutembea katika njia ndogo. [16] Nchi yao itakuwa ya hofu, kitu cha
kuzomewa milele. Kila mtu atakayepita karibu naye atashuhudia na kutingisha
kichwa chake. [17] Nitawaangamiza mbele ya adui zao kama upepo wa mashariki.
Nitawageuzia kisogo, wala sio uso wangu, siku ya msiba wao.'" [18] Basi watu
wakasema, "Njoni, tufanye njama dhidi ya Yeremia, maana sheria haitapotea kabisa
kwa makuhani, wala ushauri kutoka kwa wenye hekima, au maneno ya manabii.
Njoo, mshambulie kwa maneno yetu na tusisikilize tena chochote anachosema."
[19] Sikiliza, Ee Bwana! Na kusikiliza sauti ya adui yangu. [20] Je, maafa kutoka kwao
itakuwa malipo yangu kwa kuwa mema kwao? Kwa maana wamenichimbia shimo.
Kumbuka jinsi nilivyosimama mbele yako ili niseme mema kwa ajili yao na kugeuza
ghadhabu yako isiwapate. [21] Basi uwape watoto wao njaa, na uwatie mikononi mwa
wale wanaotumia upanga. Basi, waache wanawake wao wafiwe na kuwa wajane,
na watu wao watauawa, na vijana wao wauawe kwa upanga wa vita. [22] Kelele
ya kusikitisha isikiwe kutoka katika nyumba zao, kama utakapoleta washambuliaji
ghafla juu yao. Kwa kuwa wamechimba shimo kunikamata na wameficha mitego
katika miguu yangu. [23] Lakini wewe, Bwana, unajua mipango yao yote dhidi yangu ya
kuniua. Usisamehe uovu na dhambi zao. Usiondoe dhambi zao mbali nawe. Badala
yake, waache waangamizwe mbele yako. Tenda juu yao wakati wa ghadhabu yako.

# 19

[1] Bwana akasema hivi, "Nenda ukanunue chupa ya udongo wakati ukiwa na
wazee wa watu na makuhani. [2] Kisha uende mpaka bonde la Ben Hinomu wakati
wa kuingia kwenye mlango uliovunjika wa mfinyanzi, na huko utangaza maneno
nitakayokuambia. [3] Ukisema, 'Sikilizeni neno la Bwana, wafalme wa Yuda na wenyeji
wa Yerusalemu! Bwana wa majeshi, Mungu wa Israeli, asema hivi, "Tazameni, na
nitaletea msiba juu ya mahali hapa, na masikio ya kila mtu anayesikia yatawaka.
[4] Nitafanya hivyo kwa sababu wameniacha na kudharau mahali hapa. Katika mahali
hapa wanatoa sadaka kwa miungu mingine ambayo hawakuijua. Wao, baba zao, na
wafalme wa Yuda pia wamejaza mahali damu isiyo na hatia. [5] Walimjengea Baali
mahali pa juu na kuwachoma watoto wao kwa moto kama sadaka za kuteketezwa
kwake-kitu ambacho sijawaamuru au kutaja, wala hakuingia ndani ya akili yangu.
[6] Kwa hiyo, tazama, siku zinakuja-hili ndilo tamko la Bwana-ambapo mahali hapa
hapataitwa tena Tofethi, bonde la Ben Hinomu, kwa kuwa litakuwa bonde la

machinjo. 7 Katika mahali hapa nitatamgua mipango ya Yuda na Yerusalemu.
Nitawafanya wapate kuuawa kwa upanga mbele ya adui zao na kwa mkono wa wale
wanaotafuta maisha yao. Ndipo nitawapa miili yao kuwa chakula cha ndege wa
angani na wanyama wa dunia. 8 Ndipo nitaifanya mji huu kuwa uharibifu na kitu cha
kuzomewa, kila mtu anayepita atashangaa na kuzomea kwa sababu mateso yake yote.
9 Nitawafanya wale nyama ya wana wao na binti zao; kila mtu atakula mwili wa jirani
yake katika dhiki na katika uchungu ambao umeletwa kwao na maadui zao na wale
wanaotaka maisha yao.'" 10 Kisha utavunja chupa ya udongo mbele ya watu ambao
walikwenda pamoja nawe. 11 Uwaambie,'Bwana wa majeshi asema hivi: nitafanya
jambo hili kwa watu hawa na mji huu- hii ndiyo ahadi ya Bwana, kama vile Yeremia
alivyovunja chupa ya udongo ili isiweze kutengenezwa tena. Watu watazika wafu
huko Tofethi hata hapatabaki mahali pa kuzika. 12 Hivyo ndivyo nitakavyopafanya
mahali hapa na wenyeji wake nitakapofanya jiji hili kama Tofethi, hili ndio tamko la
Bwana; 13 kwa hiyo nyumba za Yerusalemu na wafalme wa Yuda watakuwa kama
Tofethi, nyumba zote zilizo juu ya watu waovu wanaoabudu nyota zote za mbinguni
na kumwaga sadaka za kinywaji kwa miungu mingine.'" 14 Ndipo Yeremia akatoka
Tofethi, ambako Bwana amemtuma ahubiri. Akasimama katika ua wa nyumba ya
Bwana, akawaambia watu wote, 15 "Bwana wa majeshi, Mungu wa Israeli, asema
hivi, Tazameni, nitawaletea mji huu na miji yake yote maafa yote niliyonena dhidi
yake, kwa kuwa walifanya shingo zao kuwa ngumu na kukataa kusikiliza maneno
yangu.'"

# 20

1 Pashuri, mwana wa Imeri, kuhani, alikuwa msimamizi mkuu, akamsikia Yeremia
akihubiri maneno haya mbele ya nyumba ya Bwana. 2 Basi Pashuri akampiga nabii
Yeremia, akamtia katika masanduku yaliyokuwa kwenye lango la juu la Benyamini
ndani ya nyumba ya Bwana. 3 Ikawa siku ya pili Pashuri akamtoa Yeremia nje ya
makabati. Yeremia akamwambia, "Bwana hakukuita Pashuri, lakini wewe ni Magor-
Misabibu. 4 Kwa maana Bwana asema hivi, 'Tazama, nitakufanya kuwa kitu cha
kutisha, wewe na wapendwa wako wote; kwa maana wataanguka kwa upanga wa
adui zao, na macho yako yataona. Nitawatia Yuda mkononi mwa mfalme wa Babeli.
Atawafanya kuwa mateka huko Babeli au kuwaangamiza kwa upanga. 5 Nitampa
mali zote za jiji hili na utajiri wake wote, vitu vyote vya thamani na hazina zote za
wafalme wa Yuda. Nitaweka vitu hivi mikononi mwa adui zako, nao watawakamata.
Nao watawachukua na kuwaleta Babeli. 6 Lakini wewe Pashuri, na wenyeji wote
wa nyumba yako watakwenda mateka. Utakwenda Babeli na kufa huko. Wewe
na wapendwa wako wote ambao uliwatabiria maneno ya uongo mtazikwa huko.'"
7 "Umenidanganya, Bwana. Kwa hakika nimedanganyika. Wewe ulinikamata na
kunishinda. Nimekuwa kitu cha kuchekesha. Watu wananidharau kila siku, siku
zote. 8 Kwa maana wakati wowote nimenena, nimeita na kutangaza, 'Vurugu na
uharibifu.' Na neno la Bwana limefanywa shutumu na dhihaka kwangu kila siku.
9 Nami nikisema, 'Sitafikiria juu ya Bwana tena. Sitatangaza tena jina lake.' Ni kama
moto moyoni mwangu, uliofanyika ndani ya mifupa yangu. Kwa hiyo ninajitahidi
kustahimili lakini siwezi. 10 Nimesikia habari za ugaidi kutoka kwa watu wengi
pande zote. 'Mshitaki! Lazima tumshitaki' Wale walio karibu nami kuangalia kama
nitaanguka. 'Labda anaweza kudanganywa. Ikiwa ndivyo, tunaweza kumshinda na
kujilipiza kisasi kwake.' 11 Lakini Bwana yu pamoja nami kama mpiganaji mwenye
nguvu, hivyo wale wanaonifuata watajikwaa. Hawatanishinda. Watakuwa na aibu
sana, kwa sababu hawatafanikiwa. Watakuwa na aibu ya kudumu, haitasahauliwa
kamwe. 12 Lakini wewe, Bwana wa majeshi, wewe unayemtazama wenye haki na

ambaye huona akili na moyo. Hebu nipate kuona kisasi chako juu yao kwa maana
nimekuletea shitaka langu kwako. 13 Mwimbieni Bwana! Msifuni Bwana! Kwa kuwa
ameokoa maisha ya wale waliokandamizwa kutoka kwenye mikono ya waovu. 14 Na
ilaaniwe siku niliyozaliwa. Usiruhusu siku ambayo mama yangu alinizaa ibarikiwe.
15 Na alaaniwe mtu aliyemwambia baba yangu akisema, 'Amezaliwa mtoto wa kiume,'
na kusababisha furaha kubwa. 16 Mtu huyo atakuwa kama miji ambayo Bwana
aliiangamiza bila huruma. Na asikie wito wa msaada asubuhi na sauti ya vita wakati
wa mchana. 17 Hiyo itatokea, kwa kuwa Bwana hakuniua tumboni au kumfanya
mama yangu kaburi langu, tumbo la ujauzito milele. 18 Kwa nini nilitoka tumboni ili
kuona matatizo na uchungu, ili siku zangu zijazwe na aibu?"

# 21

1 Hili ndilo neno lililotoka kwa Bwana kwa Yeremia wakati mfalme Sedekia
alimtuma Pashuri mwana wa Malkiya na Sefania mwana wa Maaseya, kuhani.
Wakamwambia, 2 "Pata ushauri kutoka kwa Bwana kwa ajili yetu, kwa kuwa
Nebukadreza, mfalme wa Babeli, analeta vita. Labda Bwana atafanya miujiza
kwetu, kama ilivyokuwa zamani, na kumfanya aondoke kwetu." 3 Basi Yeremia
akawaambia, "Hivi ndivyo mtakavyomwambia Sedekia 4 'Bwana, Mungu wa Israeli,
asema hivi: Tazama, niageuza nyuma vyombo vya vita vilivyo mkononi mwenu,
ambavyo mnapigana dhidi ya mfalme wa Babeli na Wakaldayo wanaokufunga kutoka
nje ya kuta! Kwa maana nitawakusanya katikati ya jiji hili. 5 Nami nitapigana
nanyi kwa mkono ulioinuka na mkono wenye nguvu, na ukali, ghadhabu, na hasira
kubwa. 6 Kwa maana nitawaangamiza wenyeji wa mji huu, wanadamu na wanyama,
watakufa kwa tauni kali. 7 Baada ya hayo- hii ndiyo ahadi ya Bwana-Sedekia mfalme
wa Yuda, watumishi wake, watu, na kila mtu aishiye katika mji huu baada ya tauni,
upanga na njaa, nitawatia wote mkononi mwa Nebukadreza mfalme wa Babeli, na
mikononi mwa adui zao, na katika mkono wa wale wanaotaka uhai wao. Ndipo
atawaua kwa makali ya upanga. Hatawahurumia, hatawaokoa, au kuwa na rehema.'
8 Basi uwaambie watu hawa, 'Bwana asema hivi Angalia, nitaweka mbele yako njia
ya uzima na njia ya mauti. 9 Mtu yeyote anayeishi katika mji huu atakufa kwa
upanga, njaa, na tauni; lakini mtu yeyote atakayetoka na kuanguka kwa magoti
mbele ya Wakaldayo ambao wamefungwa dhidi yako ataishi. Yeye ataokoka na
maisha yake. 10 Kwa maana nimeweka uso wangu juu ya mji huu ili kuleta maafa
na sio kuleta mema-hili ndilo tamko la Bwana. Utatiwa mkononi mwa mfalme wa
Babeli naye atauteketeza.' 11 Kuhusu nyumba ya mfalme wa Yuda, sikiliza neno la
Bwana. 12 Nyumba ya Daudi, Bwana asema, "Hukumuni kwa haki asubuhi. Umuokoe
yule aliyeibiwa kwa mkono wa mwenye kuonea, au ghadhabu yangu itatoka kama
moto na kuchoma, na hakuna mtu anayeweza kuizima, kwa sababu ya matendo yako
mabaya. 13 Angalia, mwenyeji wa bonde na mwamba wa nchi ya wazi! Mimi niko
juu yako, - hii ndiyo ahadi ya Bwana- Mimi ni juu ya mtu yeyote anayesema, 'Ni nani
atashuka kutupiga?' au 'Ni nani atakayeingia kwenye nyumba zetu?' 14 Nitawaadhibu
kutokana na matunda ya matendo yako-hili ndilo tamko la Bwana- na nitawasha moto
katika misitu, na utateketeza kila kitu.'"

# 22

1 Bwana asema hivi, "Nenda kwenye nyumba ya mfalme wa Yuda, utangaze neno
hili huko. 2 Ukaseme, 'Ewe Mfalme wa Yuda, wewe aliyeketi kiti cha Daudi, usikilize
neno la Bwana. Nisikilizeni, enyi watumishi wake, na ninyi, watu wake mnaokuja
kwa malango haya. 3 Bwana asema hivi, "Fanya haki na uadilifu, na mtu yeyote
ambaye ameibiwa-muokoeni kutoka mkononi mwa mshindani. Usimtendee mabaya
mgeni yeyote katika nchi yako, au yatima au mjane. Usifanye vurugu au kumwaga

damu isiyo na hatia mahali hapa. [4] Kwa kuwa mkifanya mambo hayo, basi wafalme
wanaoketi kiti cha Daudi wataingia milango ya nyumba hii wakiendesha gari na
farasi, yeye, watumishi wake, na watu wake! [5] Lakini ikiwa hamsikilizi maneno haya
kutoka kwangu ambayo nimeyasema-hili ndilo tamko la Bwana-basi nyumba hii ya
kifalme itaharibiwa.'” [6] Kwa maana Bwana asema hivi juu ya nyumba ya mfalme wa
Yuda, “Wewe uko kama Gileadi, au kama kilele cha Lebanoni kwangu. Hata hivyo
nitakugeuza kuwa jangwa, katika miji isiyo na wenyeji. [7] Kwa kuwa nimewaagiza
waharibifu kuja juu yenu! Watu wenye silaha zao watakata mierezi yako iliyo bora
na kuiacha kuanguka kwenye moto. [8] Kisha mataifa mengi yatapita kwenye mji huu.
Kila mtu atamwambia yule anayefuata, “Mbona Bwana amefanya hivi kwa jiji hili
kuu?” [9] Na mwingine atajibu, “Kwa sababu waliiacha agano la Bwana, Mungu wao,
wakainama kwa miungu mingine, wakaiabudu.” [10] Usilie kwa ajili ya aliyekufa.
Usiomboleze kwa ajili yake. Lakini mlilie mtu yeyote anayeingia kifungoni, kwa
maana hatarudi tena kuiona nchi aliyozaliwa.' [11] Maana Bwana asema hivi juu ya
Yehoahazi, mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda, aliyekuwa mfalme badala ya Yosia
babaye, 'ametoka mahali hapa, wala hatarudi. [12] Atakufa huko mahali ambapo
walimchukua mateka, na hataiona tena nchi hii.' [13] Ole mtu yeyote anayejenga
nyumba yake kwa uovu na vyumba vyake vya juu katika udhalimu; ambao wengine
hufanya kazi, lakini hawalipwi. [14] Ole mtu yeyote atakayesema, 'Nitajenga nyumba
ndefu na vyumba vya juu vipana, na hujenga madirisha mapana, na kuta zenye
mwerezi, na huipaka rangi nyekundu.' [15] Je, hii ndiyo inakufanya uwe mfalme mzuri,
kwamba unataka kuwa na mbao za mwerezi? Je baba yako hakula na kunywa,
lakini lakini alifanya hukumu na haki? Kisha mambo yakawa mazuri kwa ajili yake.
[16] Alihukumu maneno ya masikini na mhitaji. Ilikuwa vizuri. Je, huku siko kunijua
mimi? - hili ni tamko la Bwana. [17] Lakini hakuna kitu machoni na moyoni mwako
isipokuwa wasiwasi kwa faida yako isiyo ya haki na kwa kumwaga damu isiyo na
hatia, kwa ukandamizaji kuwatendea jeuri wengine. [18] Kwa hiyo Bwana asema
hivi juu ya Yehoyakimu, mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda. Hawatamwomboleza
wakisema 'ole, ndugu yangu! au 'Ole, dada yangu!' Hawataomboleza kwa kusema
'Ole, bwana! ' au 'ole, utukufu!' [19] Atazikwa maziko ya punda, ataburuzwa mbali
na kutupwa nje ya milango ya Yerusalemu. [20] Panda milima ya Lebanoni piga
kelele. Paza sauti yako Bashani. Piga kelele kutoka kwenye milima ya Abarimu,
kwa maana marafiki zako wote wataharibiwa. [21] Nilinena nawe wakati ulioko
salama, lakini ukasema, 'Sitasikia.' Hii ilikuwa desturi yako tangu ujana wako, kwani
hukusikiliza sauti yangu. [22] Upepo utawalisha wachungaji wako wote, na marafiki
zako watakwenda kufungwa. Hakika wewe utakuwa na aibu na kufadhaika kwa
matendo yako yote mabaya. [23] Wewe mfalme, wewe ambaye huishi katika Nyumba
ya Msitu wa Lebanoni, wewe aliyefanya kiota kati ya mierezi, utakuwa na hali ya
kuhurumiwa utakapopata utungu kama wakati wa kuzaa.” [24] “Kama mimi niishivyo-
hili ndilo tamko la Bwana-hata kama wewe, Konia, mwana wa Yehoyakimu, mfalme
wa Yuda, ulikuwa alama ya mkono wangu wa kulia, ningekuangusha. [25] Kwa kuwa
nimewatia mikono ya wale wanaotaka uhai wenu na kwenye mkono wa wale ambao
mnawaogopa, hata mkononi mwa Nebukadreza, mfalme wa Babeli na Wakaldayo.
[26] Nitawatupa wewe na mama yako aliyekuzaa katika nchi nyingine, nchi ambayo
hujazaliwa, na huko utakufa. [27] Na kuhusu eneo hili ambalo watataka kurudi,
hawatarudi hapa. [28] Je! Hiki ni chombo kilichodharauliwa na kilichopasuka? Je,
Konia ni chombo kilichodharauliwa? Kwa nini wamemtupa yeye na wazao wake,
kumpeleka katika nchi wasiyoijua? [29] Ee Ardhi, Ardhi, Ardhi! Sikieni neno la Bwana!
[30] Bwana asema hivi, 'Andika juu ya mtu huyu Konia Yeye hatakuwa na mtoto.
Hatafanikiwa wakati wa siku zake, wala hakuna hata mmoja kati ya uzao wake

atakayefanikiwa au kuketi tena kwenye kiti cha Daudi na kutawala juu ya Yuda.'”

# 23

[1] “Ole wao wachungaji ambao huangamiza na kuwatawanya kondoo wa malisho
yangu-hii ndiyo ahadi ya Bwana.” [2] Kwa hiyo, Bwana, Mungu wa Israeli, asema
hivi juu ya wachungaji ambao wanawachunga watu wake, “Ninyi mnawatawanya
kundi langu na kuwafukuza. Hamuwajali hata kidogo. Tambueni hili! Mimi
nitawalipiza uovu wa matendo yenu-hili ni tamko la Bwana. [3] Mimi mwenyewe
nitakusanya mabaki ya kondoo wangu kutoka nchi zote nilizowafukuza, nami
nitawarejesha kwenye eneo la malisho, ambako watazaa na kuongezeka. [4] Ndipo
nitawainua wachungaji juu yao ambao watawachunga hivyo hawataogopa tena au
kupotezwa. Hakuna hata mmoja atakayepotea-hili ni tamko la Bwana. [5] Angalia, siku
zinakuja-hili ndilo tamko la Bwana-nitakapomuinulia Daudi tawi la haki. Atatawala
kama mfalme; atatenda kwa busara na kusababisha hukumu na haki katika nchi.
[6] Katika siku zake Yuda ataokolewa, na Israeli wataishi kwa usalama. Na jina
lake atakayeitwa Bwana ni haki yetu. [7] Kwa hiyo, tazama, siku zinakuja-hili ndilo
tamko la Bwana-hawatasema tena, 'Kama Bwana aishivyo, aliyewatoa wana wa
Israeli kutoka nchi ya Misri.' [8] Badala yake watasema, 'Kama Bwana aishivyo,
ambaye aliwaleta na ambaye aliwaongoza wana wa nyumba ya Israeli kutoka nchi
ya kaskazini na nchi zote walizofukuzwa.' Nao watakaa katika nchi yao wenyewe.”
[9] Kuhusu manabii, moyo wangu umevunjika ndani yangu, na mifupa yangu yote
imetetemeka. Nimekuwa kama mlevi, kama mtu ambaye ameshindwa na divai,
kwa sababu ya Bwana na maneno yake matakatifu. [10] Kwa maana nchi imejaa
wazinzi. Kwa sababu ya hayo nchi imeuka. Milima katika jangwa imekauka. Njia
hizi za manabii ni mbaya; nguvu zao hazitumiwi kwa namna sahihi. [11] Kwa maana
manabii na makuhani wote wamekufuru. Nimeona uovu wao ndani ya nyumba
yangu! - hili ndilo tamko la Bwana; [12] kwa hiyo njia yao itakuwa kama mahali
pa kupumzika katika giza. Watasukumwa chini. Wao wataanguka ndani yake.
Kwa maana nitawatuma mabaya juu yao katika mwaka wa adhabu yao; hili ndilo
tamko la Bwana. [13] kwa maana nimeona uchungu kati ya manabii huko Samaria.
Walitabiri kwa Baali na wakawaongoza watu wangu Israeli kwenye njia sahihi. [14] Na
miongoni mwa manabii huko Yerusalemu nimeona mambo ya kutisha: wanafanya
uzinzi na huenda kwa udanganyifu. Wanaimarisha mikono ya waovu; hakuna
mtu anarejea na kuacha uovu wake. Wote wamekuwa kama Sodoma kwangu na
wenyeji wake kama Gomora!” [15] Kwa hiyo, Bwana wa majeshi asema hivi juu ya
manabii, “Tazameni, nitawafanya wale magugu na kunywa maji yenye sumu, kwa
maana kufuru imetoka kwa manabii wa Yerusalemu na kuingia katika nchi yote.”
[16] Bwana wa majeshi asema hivi, “Usisikilize maneno ya manabii wanaokuhubiri.
Wamekudanganya! Wanatangaza maono kutoka kwenye mawazo yao wenyewe,
si kwa kinywa cha Bwana. [17] Wanasema daima kwa wale wanaonidharau mimi,
'Bwana asema kutakuwa na amani kwako.' Na kila mtu anayetembea katika ukaidi
wa moyo wake anasema, 'mabaya hayatakuja kwenu.' [18] Lakini nani amesimama
katika mkutano wa baraza la Bwana? Ni nani anayeona na kusikia neno lake? Ni
nani anayezingatia maneno yake na kusikiliza? [19] Tazama, kuna dhoruba inayotoka
kwa Bwana! Hasira yake inatoka, na dhoruba inazunguka. Inazunguka vichwa
vya waovu. [20] Hasira za Bwana hazitarejea mpaka zitakapotimiza nia ya moyo
wake. Katika siku za mwisho, utaelewa. [21] Sikuwatuma manabii hawa. Wao tu
walionekana. Sikuwahubiri jambo lolote kwao, lakini bado wanatabiri. [22] Kwa kuwa
kama walisimama katika mkutano wangu wa baraza, wangeweza kuwasababisha
watu wangu kusikia neno langu; wangewafanya wapate kuacha maneno yao mabaya

na mazoea mabaya. 23 Mimi ni Mungu aliye karibu-hili ni tamko la Bwana-mimi
sio Mungu aliye mbali? 24 Je, kuna mtu yeyote anayejificha mahali penye siri ili
nisiweze kumwona? -Hili ndilo tamko la Bwana-Je mbingu na nchi hazikujawa nami?
-hili Ndilo tamko la Bwana. 25 Nimesikia yale waliyosema manabii, wale waliokuwa
wanatabiri uongo kwa jina langu. Wakisema, 'Nilikuwa na ndoto! 26 Nilikuwa na
ndoto!' Je, hii itaendelea mpaka lini, manabii wanaotabiri uongo kutoka kwa akili
zao, na wanasema nini kutokana na udanganyifu mioyoni mwao? 27 Wana mpango
wa kuwafanya watu wangu kusahau jina langu kwa ndoto ambazo wanazoripoti,
kila mmoja kwa jirani yake, kama vile babu zao walivyosahau jina langu kwa ajili
ya jina la Baali. 28 Nabii aliye na ndoto, aseme ndoto hiyo. Lakini yule ambaye
nimemwambia kitu fulani, basi aseme neno langu kwa kweli. Je, majani yanahusiana
na nafaka? - hili ni tamko la Bwana- 29 Na neno langu si kama moto? -Hili ni tamko
la Bwana-na kama mwamba wenye kupiga nyundo? 30 Tazameni, ninapingana na
nabii-hii ndiyo ahadi ya Bwana-yeyote anayeiba maneno kutoka kwa mtu mwingine
na anasema yanatoka kwangu. 31 Tazama, ninapingana na manabii-hili ndilo tamko
la Bwana-ambao hutumia lugha zao kutabiri maneno. 32 Tazameni, ninapingana na
manabii wanaoota ndoto-hii ndiyo ahadi ya Bwana-na kisha kuwahubiri na kwa njia
hii kuwadanganya watu wangu kwa udanganyifu wao na kujivunia. Mimi ni juu
yao, kwa kuwa sikuwatuma wala kuwapa amri. Kwa hivyo hawatawasaidia watu
hawa - hili ndilo tamko la Bwana. 33 Watu hawa au nabii au kuhani wakakuuliza,
'Je, ni nini tamko la Bwana?' basi lazima uwaambie, 'Ni tamko gani? Kwa maana
nimekuacha wewe-hili ndilo tamko la Bwana. 34 Kwa habari ya manabii, makuhani,
na watu wanaosema, 'Hili ndilo tamko la Bwana,' nitamuadhibu mtu huyo na nyumba
yake. 35 Endelea kusema, kila mtu kwa jirani yake na kila mtu kwa ndugu yake,
'Bwana alijibu nini?' na 'Bwana alitangaza nini?' 36 Lakini usizungumze tena juu
ya tamko la Bwana, kwa kuwa kila tamko kutoka kwa kila mtu limekuwa ujumbe
wake mwenyewe, na umepotosha maneno ya Mungu aliye hai, Bwana wa majeshi,
Mungu wetu. 37 Utamuuliza nabii hivi, 'Bwana alikujibu nini? Je, Bwana alisema
nini? Kisha unasema tamko kutoka kwa Bwana; 38 lakini Bwana asema hivi, Sema
hivi, "Hili ni tamko la Bwana" ingawa nimekuagiza na kusema, "Usiseme: Hili ni
tamko kutoka kwa Bwana." 39 Kwa hiyo, angalia, nitawachukua na kukutupa mbali
na mimi, pamoja na jiji ambalo nilikupa wewe na baba zako. 40 Ndipo nitaweka aibu
ya milele na fedheha juu yenu ambayo haitasahauliwa.'"

# 24

1 Bwana alinionyeshea kitu. Tazama, vikapu viwili vya tini viliwekwa mbele ya
hekalu la Bwana. (Maono haya yalitokea baada ya Nebukadreza, mfalme wa Babeli,
kumchukua mateka Yekonia mwana wa Yehoyakimu, mfalme wa Yuda, maofisa wa
Yuda, mafundi na wafua vyuma kutoka Yerusalemu na kuwapeleka Babeli.) 2 Kikapu
kimoja cha tini kilikuwa nzuri sana, kama tini za kwanza zilizoiva, lakini kikapu
kingine cha tini zilizokuwa mbaya sana zisizoweza kuliwa. 3 Bwana akaniambia,
"Unaona nini Yeremia?" Nikasema, "Tini. Tini ambazo ni nzuri sana na tini ambazo
ni mbaya sana haziwezi kuliwa." 4 Ndipo neno la Bwana likanijia, kusema, 5 "Bwana,
Mungu wa Israeli, asema hivi: nitawaangalia mateka wa Yuda kwa manufaa yao,
kama vile tini hizi nzuri, nilipowatoa mateka kutoka hapa mpaka nchi ya Wakaldayo.
6 Nitaweka macho yangu kwao wapate mema na kuwarejeshea nchi hii. Nitawajenga,
wala sitawaangamiza. 7 Nitawapanda, wala sitawang'oa. Ndipo nitawapa moyo wa
kunijua; kwa kuwa mimi ndimi Bwana. Watakuwa watu wangu na mimi nitakuwa
Mungu wao, hivyo watanirudia kwa moyo wao yote. 8 Lakini kama vile tini mbaya
ambazo ni hazifai kuliwa - asema Bwana - nitatenda hivi kwa Sedekia, mfalme

wa Yuda, pamoja na viongozi wake, na pamoja na wengine wa Yerusalemu ambao
wanabaki katika nchi hii au kwenda kukaa katika nchi ya Misri. 9 Nitawafanya kuwa
kitu cha kutisha, wapate maafa, mbele ya falme zote duniani, aibu na somo kwa
mithali, matusi, na laana mahali pote nitakapowafukuza. 10 Nitatuma upanga, njaa,
na tauni dhidi yao watapotelea mbali kutoka kwenye nchi niliyowapa wao na baba
zao."

# 25

1 Hili ndilo neno ambalo lilimjia Yeremia juu ya watu wote wa Yuda. Ikawa mwaka
wa nne wa Yehoyakimu, mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda. Huo ndio mwaka wa
kwanza wa Nebukadreza, mfalme wa Babeli. 2 Yeremia nabii aliwahubiria watu
wote wa Yuda na wenyeji wote wa Yerusalemu. 3 Akasema, "Kwa miaka ishirini na
mitatu, tangu mwaka wa kumi na tatu wa Yosia mwana wa Amoni, mfalme wa Yuda
mpaka leo, maneno ya Bwana yamekuja kwangu. Nimewahubiria ninyi. Nilikuwa
na nia ya kutangaza, lakini hamkunisikiliza. 4 Bwana akawapeleka watumishi wake
wote manabii kwako. Walikuwa na nia ya kwenda, lakini hukusikiliza wala kutega
masikio. 5 Manabaii hawa walisema, 'Kila mtu auache uovu wake na udhalimu wa
matendo yake na kurudi kwenye nchi ambayo Yahwe aliitoa wakati wa zamanai kwa
ajili ya babu zenu na ninyi, kama zawadi ya kudumu. 6 Kwa hiyo msiifuate miungu
mingine ili kuiabudu au kuiinamia chini, na msimkasirishe kwa kazi ya mikono yenu
ili kwamba awaumize. 7 Lakini hamkunisikiliza-hili ndilo tamko la Bwana-kwa hiyo
umenikasirisha kwa kazi ya mikono yako ili kujidhuru nafsi zemu. 8 Basi, Bwana wa
majeshi asema hivi, 'Kwa kuwa hukusikiliza maneno yangu, 9 tazama, nitaagiza amri
ya kukusanya watu wote wa kaskazini- asema Bwana- na Nebukadreza, mtumishi
wangu, mfalme wa Babeli, na kuwaleta juu ya nchi hii na wenyeji wake, na juu
ya mataifa yote yaliyo karibu nawe. Kwa maana nitawaangamiza. Nitawageuza
kuwa na hofu, kuwa kitu cha kuzomewa na ukiwa wa daima. 10 Sauti ya furaha na
sherehe-sauti ya bwana arusi na bibi arusi, sauti ya mawe ya kusagia na mwanga wa
taa-nitafanya mambo yote haya kutoweka kutoka kwa mataifa haya. 11 Ndipo nchi
hii yote itakuwa ukiwa na hofu, na mataifa haya watamtumikia mfalme wa Babeli
kwa miaka sabini. 12 Kisha miaka sabini itakapokamilika, nitamuadhibu mfalme
wa Babeli na taifa hilo, nchi ya Wakaldayo-hili ndilo tamko la Bwana-kwa uovu
wao na kuifanya kuwa ukiwa milele. 13 Nami nitaleta juu ya nchi hiyo maneno
yote niliyosema, na kila kitu kilichoandikwa katika kitabu hiki ambacho Yeremia
ametabiri juu ya mataifa yote. 14 Kwa maana pia mataifa mengi na wafalme wakuu
watapata watumwa kutoka mataifa haya. Nitawalipa kwa matendo yao na kazi za
mikono yao.'" 15 Kwa kuwa Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, "Chukua kikombe
hiki cha divai ya ghadhabu kutoka mkononi mwangu, ukawanyweshe mataifa yote
niliyokutuma. 16 Kwa maana watakunywa na kisha watalewa na kufanya wazimu
mbele ya upanga ambao nitaupeleka kati yao." 17 Basi, nikakichukua kikombe
mkononi mwa Bwana, nikawanywesha mataifa yote ambayo Bwana alinituma:
18 Yerusalemu, miji ya Yuda, na wafalme wake, na wakuu wake, na kuwafanya
kuwa ukiwa na kitu cha kutisha, na kuwa kitu cha kuzomewa na laana, kama ilivyo
hata leo.. 19 Mataifa mengine pia walipaswa kunywa: Farao mfalme wa Misri na
watumishi wake; maafisa wake na watu wake wote; 20 watu wote wa urithi wa
mchanganyiko na wafalme wote wa nchi ya Uzi; na wafalme wote wa nchi ya
Wafilisti, na Ashkeloni, na Gaza, na Ekroni, na mabaki ya Ashdodi; 21 Edomu na
Moabu na wana wa Amoni. 22 Wafalme wa Tiro na Sidoni, wafalme wa pwani
ng'ambo ya pili ya bahari, 23 Dedani, Tema, na Busi pamoja na wale wanyoao nywele
zao upande wa pili wa vichwa vyao, pia walipaswa kukinywa. 24 Watu hawa pia

walitakiwa kukinywa; wafalme wote wa Uarabuni na wafalme wote wa watu wa
asili mchanganyiko wanaoishi nyikani; 25 wafalme wote wa Zimri, wafalme wote
wa Elamu, na wafalme wote wa Wamedi; 26 wafalme wote wa kaskazini, wale wa
karibu na wale wa mbali—kila mmoja na ndugu zake na falme zote za ulimwengu
ambazo ziko chini ya uso wa dunia. Hatimaye mfalme wa Babeli atakunywa baada
yao wote. 27 Bwana akaniambia, "Basi, uwaambie, 'Bwana wa majeshi, Mungu wa
Israeli, asema hivi kunywa na kulewa, kisha tapika, uanguke, wala usisimame mbele
ya upanga nitakaoutuma kati yenu.' 28 Kisha itatokea kwamba ikiwa wanakataa
kuchukua kikombe mkononi mwako ili kunywa, utawaambia, 'Bwana wa majeshi
asema hii lazima mnywe. 29 Kwa maana, tazama, nitaleta janga juu ya mji ulioitwa
kwa jina langu, je ninyi mtaachiliwa msiadhibiwe? Hutakuwa huru, kwa maana
nitaita upanga juu ya wenyeji wote wa nchi! - ndilo tamko la Bwana wa majeshi.'
30 Basi wewe mwenyewe, Yeremia, tabiri kwao maneno haya yote. Uwaambie, 'Bwana
atanguruma kutoka juu, naye atapaza sauti yake toka makao yake matakatifu, na
radi kutoka mahali pake patakatifu; naye atapiga kelele kama wale wakanyagao
zabibu dhidi ya wote wanaoishi duniani. 31 Kelele huja mpaka mwisho wa nchi,
kwa sababu mgogoro kutoka kwa Bwana utaleta mashtaka dhidi ya mataifa. Ataleta
haki kwa wote wenye mwili. Yeye atawatia waovu katika upanga-hili ndi'o tamko
la Bwana.' 32 Bwana wa majeshi asema hivi, 'Tazameni, taabu itatokea toka kwa
taifa hadi taifa, na dhoruba kubwa itatokea toka pande za mwisho za dunia. 33 Kisha
wale waliouawa na Bwana watakuja kutoka upande mmoja wa dunia hadi mwingine;
hawataomboleza, kukusanyika, au kuzikwa. Watakuwa kama samadi chini. 34 Pigeni
Yowe, wachungaji, na pigeni kelele ya kuomba msaada! Gaagaa katika ardhi,
enyi mlio hodari katika kundi. Kwa kuwa siku yako ya kuuawa na kutawanywa
imekuja. Utaanguka kama kondoo waliochaguliwa. 35 Wachungaji hawatakuwa na
pa kukimbilia. Hakuna kutoroka kwa watu walio hodari katika kundi. 36 Kuna mlio
wa wasiwasi wa wachungaji na milio ya kulalama kwa watu walio hodari katika
kundi, kwa kuwa Yahweh anayaharibu malisho yao. 37 Kwa hiyo, malisho ya amani
yataharibiwa kwa sababu ya hasira ya Bwana. 38 Kama simba, ameacha shimo lake,
kwa kuwa ardhi yao itakuwa kitu cha kushangaza kwa sababu ya hasira ya muonevu,
kwa sababu ya ghadhabu yake kali'"

# 26

1 Mwanzoni mwa utawala wake Yehoyakimu mwana wa Yosia, neno likaja kutoka
kwa Yeremia, likisema, 2 "Yahwe anasema hivi: Simama katika uwanja wa nyumba
yangu na sema kuhusu miji yote ya Yuda ambao huja kuabudu katika nyumba
yangu. Tangaza maneno yote niliyokuamuru kuyasema kwao. Usipunguze neno
lolote! 3 Labda watasikiliza, kwamba kila mtu ataziacha njia zake mbaya, ili nighairi
majanga ninayokusudia kuyaleta juu yao kwa sababu ya uovu wa matendo yao.
4 Kwa hiyo lazima useme kwao, 'Yahwe anasema hivi: Kama hamtanisikiliza ili
mtembee katika sheria yangu ambayo nimeiweka mbele yenu— 5 kama hamsikilizi
maneno ya watumishi wangu manabii ambao naendelea kuwatuma kwenu—lakini
hamjasikiliza! — 6 kisha nitaifanya nyumba hii kuwa kama Shilo; nitaifanya nyumba
hii kuwa laana katika macho ya mataifa yote juu ya dunia. 7 Makuhani, manabii,
na watu wote wakamsikia Yeremia akitangaza maneno haya katika nyumba ya
Yahwe. 8 Kwa hiyo ikatokea kwamba Yeremia alipomaliza kutangaza aliyokuwa
Yahwe alimwwamuru kuyasema kwa watu wote, makuhani, manabii, na watu wote
wakamsimamisha na kusema, "Hakika utakufa! 9 Kwa nini umetabiri katika jina
la Yahwe na kusema kwamba nyumba hii itakuwa kama Shilo na mji huu utakuwa
ukiwa, pasipo wakaaji?" Kwa maana watu wote wameunda kundi dhidi ya nyumba

ya Yeremia. [10] Kisha wakuu wa Yuda wakasikia maneno haya na wakapanda
kutoka nyumba ya mfalme kwenda kwenye nyumba ya Yahwe. Wakakaa katika
njia ya lango katika Lango Jipya la nyumba ya Yahwe. [11] Makuhani na manabii
wakasema kwa wakuu wa Yuda na kwa watu wote. Wakasema, “Ni haki kwa mtu
huyu kufa, kwa maana ametabiri juu ya mji huu, kama mlivyosikia kwa masikio
yenu!” [12] Kwa hiyo Yeremia akasema kwa wakuu wote na watu wote, “Yeremia
amenituma kutabiri juu ya nyumb hii na mji wake, kusema maneno yote ambayo
mmeyasikia. [13] Kwa hiyo sasa, imarisheni njia zenu na matendo yenu, na sikilizeni
sauti ya Yahwe Mungu wenu kwamba ataghairi kuhusu janga ambalo ametangaza
dhidi yenu. [14] Mimi mwenyewe—niangalieni! —niko mikononi mwenu. Nitendeeni
yaliyo mema na sahihi katika macho yenu. [15] Lakini kwa hakika lazima mjue
kwamba kama mtaniua mimi, basi mnaiweka damu isiyo na hatia juu yenu wenyewe
na juu ya mji huu na wakaaji wake, kwa maana Yahwe amenituma kweli kwenu
ili nitangaze maneno yote kwa ajili ya masikio yenu.” [16] Kisha wakuu na watu
wote wakasema kwa makuhani na manabii, “Si vyema kwa mtu huyu kufa, kwa
maana ametangaza mambo haya kwetu katika jina la Yahwe Mungu wetu.” [17] Kisha
watu kutoka wazee wa nchi wakasimama na kusema kwa kusanyiko lote la watu.
[18] Wakasema, “Mikaya Mmorashi alikuwa akitabiri katika siku za Hezekia mfalme wa
Yuda. Alinena kwa watu wote wa Yuda na kusema, 'Yahwe wa majeshi anasema hivi:
Sayuni utalimwa kama shamba, Yerusalemu utakuwa lundo la magofu, na mlima wa
hekalu utakuwa kilima kilichoota vichaka.' Hezekia mfalme wa Yuda na Yunda wote
walimuua? [19] Hakumwogopa Yahwe na kuutaka radhi uso wa Yahwe ili kwamba
Yahwe angeghairi kuhusu janga ambalo alilitangaza kwao? Kwa hiyo tutafanya
maovu makubwa zaidi juu ya maisha yetu sisi wenyewe?” [20] Wakati huo huo
palikuwa na mtu mwingine ambaye alitabiri katika jina la Yahwe—Uria mwan wa
Shemaya kutoka Kiriath Yearimu—pia alitabiri juu ya mji na nchi hii, akikubaliana
na maneno yote ya Yeremia. [21] Lakini Mfalme Yohoyakimu na wanajeshi wake wote
na watumishi wake wote waliposikia maneno yake, kisha mfalme alijaribu kumuua,
lakini Uria alisikia na kuogopa, kwa hiyo alikimbia na akaenda Misiri [22] Kisha mfalme
Yehoyakimu alituma watu kwenda Misiri—Elnathani mwana wa Achbori na watu
kwenda Misiri kumfuata Uria. [23] Wakamtoa Uria nje kutoka Misiri na kumleta kwa
Mfalme Yehoyakimu. Kisha Yehoyakimu akamuua kwa upanga na kumpeleka nje
kwenye makaburi ya watu wa kawaida. [24] Lakini mkno wa Ahikamu mwana wa
Shapni alikuwa pamoja na Yeremia, hivyo hakutiwa mikonono mwa watu ili auawe.

## 27

[1] Katika mwanzo wa utawala wa Sedekia mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda,
neno hil lilimjia Yeremia kutoka kwa Yahwe. (Ingawa nakala nyingi za Kiebrania
zinasema “Yehoyakimu, matoleo mengi ya kisasa yanasema “Sedekia”, kwa sababu
tukio katika sura hii lilitokea katika kipindi cha utawala wake). [2] Hiki ndicho
Yahwe alisema kwangu, “Tengeneza vifungo na nira kwa ajili yako mwenyewe.
Ziweke shingoni mwako. [3] Kisha akawatuma kwenda kw mfalme wa Edomu,
mfalme wa Moabu, mfalme wa watu wa amoni, mfalme wa Tiro, na kwa mfalme
wa Sidoni. Watume kwa mkono wa wajumbe hao wa wafalme ambao walikuja
Yerusalemu kwa Sedekia mfalme wa Yuda. [4] Toa amri kwao kwa ajili ya mabwana
zao na sema, ' Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: Hivyo ndivyo
utakavyosema kwa mabwana zenu, [5] Mimi mwenyewe niliiumba dunia kwa nguvu
zangu kuu na mkono wangu ulioinuka. Pia niliwaumba watu na wanyama juu ya
dunia, na nikawatoa kwa yeyote aliyesahihi katika macho yangu. [6] Kwa hiyo sasa,
Mimi mwenyewe naziweka nchi hizi zote kwenye mkono wa Nebukadreza, mfalme

wa Babeli, mtumishi wangu. Pia, ninavikabidhi kwake viumbe hai vyote katika
mashamba ili vimtumikie. 7 Kwa maana mataifa yote watamtumikia yeye, wanaye, na
wajukuu zake hadi muda wa nchi yake ufike. Kisha mataifa mengi na wafalme wengi
watamtiisha. 8 Kwa hiyo taifa na ufalme ambo haumtumikii Nebukadreza, mfalme
wa Babeli, na ule usioweka shingo yake chini ya nira ya Nebukadreza mfalme wa
Babeli—nitaliadhibu taifa hilo kwa upanga, njaa, na pigo—hili ni tangazo la Yahwe—
hadi nitakapokuwa nimewateketeza kwa mkono wake. 9 Kwa hiyo msiwasikilize
manabii wenu, wabashiri wenu, waonaji wenu, ndoto zenu, watambuzi wenu,
ambao wamekuw wakisema kwenu na kusema, ' Msimtumikie mfalme wa Babeli.'
10 Kwa maana wanatabiri uongo kwenu ili kuwapeleka mbali na nchi zenu, kwa
maana nitawapeleka mbali, na mtakufa. 11 Lakini taifa ambalo wataweka shingo
zao chini ya nira ya mfalme wa Babeli na kumtumikia, nitawaruhusu kupumzika
katika nchi yao—hili ni tangazo la Yahwe—na watailima na kufanya nyumba zao
humo."" 12 Kwa hiyo nilisema kwa Sedekia mfalme wa Yuda na kumpa ujumbe
huu, "Ziwekeni shingo zenu chini ya nira ya mfalme wa Babeli na mtumikieni yeye
na watu wake, na mtaishi. 13 Kwa nini mfe—wewe na watu wako—kwa upanga,
njaa, na pigo, kama vile nilivyotangaza kuhusu taifa ambalo watapuuza kumtumikia
mfalme wa Babeli? 14 Msisikilize maneno ya manabii wanaozungumza kwenu na
kusema, 'Msimtumikie mfalme wa Babeli', kwa maana wanatabiri uongo kwenu.
15 'Kwa maana mimi sikuwatuma—hili ni tangazo la Yahwe—kwa maana wanatabiri
uongo katika jina langu ili kwamba niwafukeze inje na muangamie, ninyi nyote
na manabii wanaotabiri kwenu."' 16 Nilitangaza hili kwa makuhani na watu wote
na kusema, "Yahwe anasema hivi: Msisikilize maneno ya manabii wanaotabiri
kwenu na kusema, 'Angalia! Vyombo vya nyumba ya Yahwe vinarudishwa kutoka
Babeli sasa hivi!' Wanatabiri uongo kwenu. 17 Msiwasikilize. Mtamtumikia mfalme
wa Babeli na mtaishi. Kwa nini mji huu uangamizwe? 18 Kama ni manabii, na
kama neno la Mungu limekuja kwao kweli, basi wamwombe Yahwe wa majeshi
asivipeleke Babeli vyombo vilivyosalia katika nyumba, nyumba ya mfalme wa Yuda,
na Yerusalemu. 19 Yahwe wa majeshi anasema hivi kuhusu zile nguzo, bahari,
na kitako, na vyombo vyote vilivyosalia katika mji huu— 20 vyombo ambavyo
Nebukadreza mfalme wa Babeli hakuvichukua wakati alipomchukua Yekonia mwana
wa Yehoyakimu, mfalme wa Yuda, katika utumwa kutoka Yerusalemu kwenda Babeli
pamoja na wakuu wote wa Yuda na Yerusalemu. 21 Yahwe wa majeshsi, Mungu wa
Israeli, anasema hivi kuhusu vyombo vilivyosalia katika nyumba ya Yahwe, nyumba
ya mfalme wa Yuda, na Yerusalemu, 22 'Vitaletwa Babeli, na vitabaki huko hadi
siku niyovipangia kutimia—hili ni tangazo la Yahwe—kisha nitavileta na kuvirudisha
kataika sehemu hii."

# 28

1 Ilitokea katika mwaka ule, mwanzoni mwa utawala wa Sedekia mfalme wa Yuda,
katika mwaka wa nne na mwezi wa tano, Hanania mwana wa Azuri nabii, alikuwa
wa Gibeoni, alisema kwangu katika nyumba ya Yahwe mbele za makuhani na watu
wote. Alisema, 2 "Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: Nimeivunja
nira iliyowekwa na mfalme wa Babeli. 3 Ndani ya miaka miwili nitavirudisha
katika sehemu hii vyombo vyote vya nyumba ya Yahwe ambavyo Nebukadreza
mfalme wa Babeli livichukua kutoka sehemu hii na kuvisafirisha hadi Babeli. 4 Kisha
nitawarudisha katika sehemu hii Yekonia mwana wa Yehotakimu, mfalme wa Yuda,
na mateka wote wa Yuda ambao walipelekwa Babeli—hili ni tangazo la Yahwe—kwa
maana nitaivunja nira ya mfalme wa Babeli." 5 Kwa hiyo Yeremia nabii akasema kwa
Hanania nabii mbele ya makuhani na kwa watu wote waliosimama katika nyumba ya
Yahwe. 6 Yeremia nabii akasema, "Yahwe afanye hivi! Yahwe ayathibitishe maneno

ambayao ulitabiri na kuvirudisha katika sehemsu hii vyombo vya nyumb a ya Yahwe,
na mateka wote kutoka Babeli. 7 Vile vile, sikilizeni neno ambaloo ninalitangaza
katika masikio yenu na katika masikio ya watu wote. 8 Manabii ambao walikuwepo
mbele yangu na na mbele yenu muda mrefu uliopita pia walitabiri kuhusu mataifa
mengi na juu ya falme kuu, kuhusu vita, njaa, na mapigo. 9 Kwa hiyo nabii anayetabiri
kwamba kutakuwa na amani—kama neno lake litatimia, basi itajulikana kwamba
yeye ni nabii kweli aliyetumwa na Yahwe." 10 Lakini Hanania nabii akaichukua nira
kutoka kwenye shingo ya Yeremia na kuivunja. 11 Kisha Hanania akanena mbele
ya watu wote na kusema, "Yahwe anasema hivi: Kama hivi tu, ndani ya miaka
miwili nitaivunja nira iliyowekwa na Nebukadreza mfalme wa Babeli kutoka kwenye
shingo ya kila taifa." Kisha Yeremia nabii akaenda njia yake. 12 Baada ya Hanania
nabii kuivunja nira kutoka kwenye shingo ya Yeremia nabii, neno la Yahwe likamjia
Yeremia. likisema, 13 Nenda na ukaseme kwa Hanania na useme, Yahwe anasema
hivi: Uliivunja nira ya mbao, lakini badala yake nitafanya nira ya chuma.' 14 Kwa
maana Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi: Nimeweka nira ya chuma
shingoni mwa mataifa haya yote ili wamtumikea Nebukadreza mfalme wa Babeli,
na watamtumikia. Pia nimempa wanyama wa mashambani awatawale." 15 Kisha
nabii Yeremia akamwambia Hanania nabii, "Sikiliza Hanania! Yahwe hajakutuma,
bali wewe mwenyewe umewasababisha watu hawa kuamini katika uongo. 16 Kwa
hiyo Yahwe anasema hivi: Angalia, niko karibu kukutuma nje ya dunia. Mwaka huu
utakufa." 17 Katika mwezi wa saba wa mwaka ule ule, Hanania nabii akafa.

# 29

1 Haya ni maneno katika waraka ambao Yeremia nabii alituma kutoka Yerusalemu
kwa wazee waliosalia miongoni mwa mateka na makuhuni, manabii, na watu
wote ambao Nebukadreza aliwapeleka utumwani kutoka Yerusalemu hadi Babeli.
2 Hii ilikuwa baada ya Yekonia mfalme, mama yake mfalme, na watumishi wakuu,
viongozi wa Yuda na Yerusalemu, na wahunzi walikuwa wamepelekwa mbali na
Yerusalemu. 3 Aliutuma waraka huu kwa mkono wa Elasa mwana wa Shafani,
Gemaria, mwana wa Hilkia, ambaye Sedekia, mfalme wa Yuda, alikuwa amemtuma
kwa Nebukadreza mfalme wa Babeli 4 Waraka ulisema, Yahwe wa majeshi, Mungu
wa Israeli, anasema hivi kwa mateka ambao niliwasababisha kuwa mateka kutoka
Yerusalemu hadi Babeli, 5 'Jengeni nyumba na muishi ndani yake. Pandeni bustani
na mle matunda yake. 6 Chukueni wake na mzae wana na mabinti. Kisha Kisha
chukueni wake kwa ajili ya wana wenu, na wapatieni waume binti zenu. Wazae
wana na mabinti na waongezeke ili msiwe wachache sana. 7 Itafuteni amani ya
mji ambako nimewafanya kuwa watumwa, na mkauombee kwangu kwa niaba yake
kwa kuwa kutakuwa na amani kwenu kama mji uko katika amani.' 8 Kwa maana
Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi, 'Msiwaache manabii ambao
wako katikati yenu na wabashiri wenu kuwadanganya, na msizisikilize ndoto ambazo
ninyi wenyewe mnaota. 9 Kwa maana wanatabiri uongo kwenu katika jina langu.
Mimi sikuwatuma—hili ni tangazo la Yahwe.' 10 Kwa maana Yahwe anasema hivi,
'Babeli atakapokuwa amewatawala kwa muda wa mika sabini, nitawasaidia ninyi
na kulitimiza neno langu jema kwa ajili yenu ili kuwarudisha ninyi katika sehemu
hii. 11 Kwa maana mimi mwenyewe naijua mipangao niliyonayo kwa ajili yenu—
hili ni tangazo la Yahwe—mipango kwa ajili ya amani na siyo kwa ajili ya mabaya,
ili kuwapa ninyi tumaini na siku zenu za mwisho. 12 Kisha mtaniita, na kwenda
na kuniomba mimi, na nitawasikiliza. 13 Kwa maana mtanitafuta na kunipata,
kwa kuwa mtanitafuta kwa moyo wenu wote. 14 Kisha nitapatikana kwenu—hili
ni tangazo la Yahwe—na nitawarudisha watu wenu waliofungwa; nitawakusanya

kutoka mataifa yote na sehehemu zote ambako nimewatawanya—hili ni tangazo la
Yahwe—kwa maana nitawarudisha kutoka sehemu ambako niliwasababisha kuwa
mateka. 15 Tangu mliposema kwamba Yahwe ameinua manabii kwa ajili yetu katika
Babeli, 16 Yahwe anasema hivi kwa mfalme aliyeketi katika kiti cha enzi cha Daudi na
watu wote wakaao katika mji huo, ndugu zenu ambao hawakwenda pamoja nanyi
utumwani— 17 Yahwe wa majeshi anasema hivi, ''Ona, niko karibu kutuma upanga,
njaa, na ugonjwa juu yao. Kwa maana nitawafanya kuwa kama tini mbovu ambazo
ni mbaya sana hazifai kuliwa. 18 Kisha nitawafuata kwa upanga, njaa, na tauni
na kuwafanya kuwa kitu cha kushangaza kwa falme zote juu ya dunia—kitu cha
kuogofya, kitu cha kulaaniwa na kuzomewa, na kitu cha aibu miongoni mwa mataifa
yote ambako nilimtawanya. 19 Hii ni kwa sababu hawakulisikiliza neno langu—hili
ni tangazo la Yahwe—ambalo nililituma kwao kupitia watumishi wangu manabii.
Niliwatuma tena na tena, lakini hamkusikiliza—hili ni tangazo la Yahwe. ' 20 Kwa
hiyo ninyi wenyewe sikilizeni neno la Yahwe, ninyi mateka wote ambao amewatuma
kutoka Yerusalemu hadi Babeli, 21 'Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema
hivi kuhusu Ahabu mwana wa Kolaya na Sedekia mwana wa Maaseya, watabirio
uongo kwenu katika jina langu: Ona, niko karibu kuwaweka katika mkono wa
Nebukadreza mfalme wa Babeli. Atawaua mbele ya macho yenu. 22 Kisha laana
itatamkwa na wafungwa wote wa Yuda katika Babeli kuhusu watu hawa. Laana
itasema: Yahwe awafanye kuwa kama Sedekia na Ahabu, ambao mfalme wa Babeli
aliwaoka kwenye moto. 23 Hili litatokea kwa sababu ya mambo ya aibu waliyofanya
katika Israeli walipofanya uzinzi na wake za majarani zao na kutangaza maneno
ya uongo katika jina langu, mambo ambayo sikuwaamuru wayaseme. Kwa maana
mimi ndiye nijuaye; mimi ni shahidi—hili ni tangazo la Yahwe."' 24 Kuhusu Shemaya
Mnehelami, sema hivi: 25 'Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi:
Kwa sababu ulituma barua kwa jina lako kwa watu wote katika Yerusalemu, kwa
Sefania mwana wa Maaseya kuhani, na kwa makuhani wote, na ulisema, 26 "Yahwe
aliwafanya ninyi kuwa makuhani badala ya Yehoyada kuhani, ili muwe wasimamizi
wa nyumba ya Yahwe. Ninyi ni viongozi wa watu wote wajitiao wazimu na kujifanya
wenyewe manabii. Mtawaweka katika mkatale na minyororo. 27 Kwa hiyo sasa,
kwa nini hamkumkemea Yeremia wa Anathothi, ambaye hujifanya mwenyewe nabii
juu yenu? 28 Kwa maana ametutumia sisi katika Babeli, 'Itakuwa muda mrefu.
Jengeni nyumba na muishi ndani yake, na pandeni busitani na mule matunda yake.""
29 Sefania kuhani akaisoma barua hii mbele ya Yeremia nabii. 30 Kisha neno la Yahwe
likaja kwa Yeremia, likisema, 31 "tuma neno kwa mateka wote na sema, 'Yahwe
anasema hivi kuhusu Shemaya Mnehelami: Kwa sababu Shemaya amewatabiria
ninyi wakati mimi sikumtuma, na amewaongoza kuamini uongo, 32 kwa hiyo Yahwe
anasema hivi: Angalia, niko karibu kumwadhibu Shemaya Mnehelami na uzao wake.
Hapatakuwa na mtu wa kukaa miongoni mwa watu hawa kwa ajili yake. Hataona
mema nitakayofanya kwa ajili ya watu wangu—hili ni tangazo la Yahwe—kwa maana
ametangaza uasi dhidi ya Yahwe.""

# 30

1 Neno lilokuja kwa Yeremia kutoka kwa Yahwe likisema, 2 "Hivi ndivyo Yahwe,
Mungu wa Israeli, anasema, 'Jiandikie mwenyewe katika baraua maneno yote
niliyotangaza kwako katika barua. 3 Maana ona, siku zinakuja—hili ni tangazo la
Yahwe—nitakapowarudisha mateka wa watu wangu Israeli na Yuda. Mimi, Yahwe,
nimesema hili. Kwa maana nitawarudisha kwenye nchi ambayo niliwapa babu zao,
na wataimiliki."' 4 Haya ni maneno ambayo Yahwe anatangaza kuhusu Israeli na
Yuda, 5 "Kwa maana Yahwe anasema hivi, 'Tumesikia sauti ya kutetemesha ya hofu

na wala siyo ya amani. [6] Ulizeni na muone kama mwanaume anamwogopa mtoto.
Mbona ninamwona kila mwanaume kijana ameshika mikono yake juu ya kiuno chake
kama mwanamke anayejifungua mtoto? Kwa nini nyuso zao wote zimegeuka rangi?
[7] Ole! Kwa maana siku hiyo itakuwa kuu, isiyofanana na yoyote. Utakuwa wakati
wa huzuni kwa Yakobo, lakini ataokolewa. [8] Kwa maana itakuwa katika siku hiyo—
hili ni tangazo la Yahwe wa majeshi—kwamba nitaivunja nira ya shingo zenu, na
nitaisambaza minyororo yenu, kwa hiyo wageni hawatawafanya watumwa tena.
[9] Bali watamwabudu Yahwe Mungu wao na kumtumikia Daudi mfalme wao, ambaye
nitamfanya mfalme juu yao. [10] Kwa hiyo wewe, mtumishi wangu Yakobo, usiogope—
hili ni tangazo la Yahwe—na usikate tamaa, Israeli. Maana ona, niko karibu
kukurudisha kutoka mbali, na uzao wako kutoka nchi ya utumwa,. Yakobo atarudi
na kuwa katika amani; ataokolewa, na hapatakuwa na hofu zaidi. [11] Kwa maana niko
pamoja nawe—hili ni tangazo la Yahwe—ili kukuokoa. Kisha nitaleta mwisho kamili
kwa mataifa yote ambako nimewatawanya. Bali sitaweka mwisho kwako, ingawa
ninakuadhibu kwa haki na kwa hakika sitakuacha bila kukuadhibu.' [12] Kwa maana
Yahwe anasema hivi, 'Jeraha lako si la kupona; kidonda chako kimeenea. [13] Hakuna
mtu wa kukutetea kesi yako; hakuna utetezi kwa ajili ya kidonda chako ili upone.
[14] Wapenzi wako wote wamekusahau. Hawatakuangalia, kwa maana nimekujeruhi
kwa jeraha la adui na nidhimu ya bwana mkatili kwa sababu ya uovu wako mwingi
na dhambi zako zisizohesabika. [15] Kwa nini unaita msaada kwa ajili ya jeraha lako?
Maumivu yako hayaponyeki. kwa sambabu ya uovu wako mwingi, dhambi zako
zisizohesabika, nimefanya mambo haya kwako. [16] Kila mtu akulaye ataliwa, na adui
zako wote wataenda utumwani. Kwa maana kila aliyekuteka nyara atatekwa, na
nitawafanya wote wanaokuwinda kuwa mawindo. [17] Kwa maana nitaleta uponyaji
juu yako; nitakuponya majeraha yako—hili ni tangazo la Yahwe—nitafanya hivyo
kwa sababu walikuita: Mwenyekutupwa. Hakuna anayeujali Sayuni." [18] Yahwe
anasema hivi, "Ona, niko karibu kuwarudisha mateka wa hema za Yakobo na
kuwa na huruma juu ya nyumba zake. Kisha mji utajengwa juu ya lundo la
magofu, na jumba litakuwepo tena kama ilivyokuwa kawaida. [19] Kisha wimbo wa
kusifu na sauti ya ya shangwe itasikika kutoka kwao, kwa maana nitawaongeza na
wala sitawapunguza; nitawaheshimu ili kwamba wasifanywe wanyonge. [20] Kisha
watu watakuwa kama ilivyokuwa mwanzo, na kusanyiko lao litaanzishwa mbele
yangu wakati nitakapowaadhibu wote wanaowatesa kwa sasa. [21] Kiongozi wao
atatoka miongoni mwao. Atatokeza kutoka kati yao nitakapomleta karibu na
atakapanikaribia mimi. kama sitafanya hivyo, ni nani atakayethubutu kunisogelea?
—hili ni tangazo la Yahwe. [22] Kisha mtakuwa watu wangu, na nitakuwa Mungu
wenu. [23] Ona, tufani ya Yahwe, ghadhabu yake, imekwenda nje. Ni tufani isiyokoma.
Itazunguka juu ya vichwa vya watu waovu. [24] Hasira ya Yahwe haitarudi mpaka
itoke na kutimiza makusudi ya moyo wake. Katika siku za mwisho mtalielewa hili."

# 31

[1] "Katika wakati huo—hili ni tangazo la Yahwe—Nitakuwa Mungu wa familia
zote za Israel, na watakuwa watu wangu." [2] Yahwe anasema hivi, "Watu ambao
wamenusurika na upanga wamepata kibali katika nyika; nitatoka nje kuwapa
pumziko Israeli." [3] Yahwe alionitokea zamani na kusema, "Nimekupenda wewe,
Israeli, kwa upendo wa milele. Kwa hiyo nimekuvuta kwang kwa agano la uaminifu.
[4] Nitakujenga tena kwa hiyo utakuwa umejengwa, bikra wa Israeli..... na kwenda
nje michezo ya furaha. [5] Utapanda mizabibu tena juu ya milima Samaria; wakulima
watatapanda na kuweka matunda kwa ajili ya matumizi mazuri. [6] Kwa maana siku
itakuja wakati walizi watakapotangaza katika milima ya Efraimu, 'Inuka, twndeni

juu kwenye mlimaa wa Yahwe Mungu wetu.' 
7 Kwa maana Yahwe anasema hivi,
Piga kelele za shangwe juu ya Yakobo! Pigeni za furaha kwa ajili ya watu wakuu
wa mataifa! Sifa zisikike. Sema, ''Yahwe amewaokoa watu wake, masalia wa
Israeli.' 
8 Ona, niko karibu kuwaletaa kutoka nchi za kusini. Nitawakusanya kutoka
sehemu zaa mbali za dunia. Vipofu na wenye ulemavu watakuwa kati kati yao;
wanawake wajawazito na wale waliokaribu kujifungua wataakuwa pamoja nao.
Kusanyiko kubwa litarudi hapa. 
9 Watakuja kwa kuomboleza; nitawaongoza huku
wakifanya maoambi yao. Nitawafanya wasafiri kataika mikondo ya maji katika bara
bara ilinyoka. Hawatajikwaa juu yake, kwa maana nitakuwa baba kwa Israeli, na
Afraimu atakuwa mzaliwa wanagau wwa kwanza 
10 Sikia neno la Yahwe, mataifa.
Litangazeni pembezoni mwa visiwa mbali. Enyi mataifa lazima museme, 'Yule
aliyemtawanya Israeli anamkusanya tena na kuwalinda kama mchungaji alindavyo
kondoo.' 
11 Kwa maana Yahwe amemfidia Yakobo na kumkomboa kutoka mkono
ambao ulikuwa na nguvu sana kwake. 
12 Kisha watakuja na kufurahia katika vilele
vya Sayuni. Nyuso zao zitamelemeta kwa sababu ya wema wa Yahwe, juu ya nafaka
na divai mpya, juu ya mafuta na malimbuko ya kwanza ya makundi na ng'ombe.
Kwa maana maisha yao yatakuwa kama busitani iliyomwagiliwa, na hatatajisikia
huzuni tena. 
13 Kisha wanawali watafurahia kwa kucheza, na vijana na wanaume
wazee watakuwa pamaoja. Kwa maana nitayageuza maombolezo yao kuwa sherehe.
Nitakuwa na huruma juu yao na kuwafanya kufurahi badala ya kuhuzunika. 
14 Kisha
nitayaloanaisha sana maisha ya makuhani. Watu wangu watajijaza wenyewe kwa
wema—hili ni tangazo la Yahwe.” 
15 Yahwe anasema hivi: “Sauti imesikika katika
Rama, kilio na maombolezo mengi. Ni Raheli akiomboleza kwa ajili watoto wake.
Hataki kufarijiwa tena juu yao, kwa maana hawako hai tena.” 
16 Yahwe anasema
hivi, Zuia sauti yako usilie na macho yako yasitoe machizi; kwa maana kuna fidia
kwa ajili ya mateso yako—hili ni tangazo la Yahwe—watoto wako watarudi kutoka
nchi ya adui. 
17 Kuna matumaini kwa ajili ya siku zenu za baadaye—hili ni tangazo
la Yahwe—uzao wako watarudi ndani ya mipaka yao.” 
18 Kwa hakika nimemsikia
Efraimu akilia, 'Uliniadhibu, nami nieadhibika kama ndama assiye na mafunzo.
Nirudisha na nitarudishwa, kwa maana wewe ni Yahwe Mungu wangu. 
19 Kwa
maana baada ya kurudi kwako, nilikuwa na huzuni; baada ya kufundiswa, nilijipiga
kofi sshavu langu. Niliaibika ana dharirika, kwa maana nilizaliwa na hataia ya
ujana wangu.' 
20 Efraimu siyo mtoto wangu wa thamani? Yeye si mpendwa wangu,
mwanangu anipendezaye? Kwa maana kila ninaponena juu yake, bado nina mwita
kipenzi cha akili yangu. Kwa namna hii moyo wangu unamtamani. Kwa hakika
nitaakuwa na huruma ajuu yake—hili ni tangazo la Yahwe.” 
21 Jiwekee alama za
bara bara kwa ajili yako mwenyewe. Weka matangaazo ya maelekezo kwa ajili
yako mwenyewe. Iweke akili yako juu ya njia sahihi, njia unayopaswa kufuata.
Rudii, bikra Israeli! Rudi kwenye hii miji yako. 
22 Utatanga tanga hadi lini, binti
usiye mwaminifu? Kwa maana Yahwe ameumba kitu fulani kipya juu ya dunia—
mwanamke anamzunguka mwanaume. 
23 Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli,
anasema hivi, '“Nitakapowarudisha watu katika nchi yao, watasema hivi katika anchi
ya Yuda na miji yake, “Yahwe akubariki, wewe sehemu takatifu ambapo anaishi,
ewe mlima mtakatifu.' 
24 Kwa maana Yuda na miji yake yote wataishi pamoja humo,
kama vile watakavyoishi wakulima na wachungaji pamaoja na makundi yao. 
25 Kwa
maana nitawapa majai ya kunywa waliochoaka, na nitamjaza kila anayeteseka na
kiu.” 
26 Baada ya haya niliamka, na nikagundua kwamba usingizi wangu ulikuwa
unaburudisha. 
27 Angalia, siku zinakuja—hili ni tangazo la Yaahwe—nitakapoipanda
nyumba ua Israeli na Yuda pamoja na wazawa wa wanadamaau na wanyama.
28 Zamani, niliwaweka katika uangalizi ili kuwang'oa na kuwabomoa, kuwaangusha,

kuwaharibu, na kuwaletea madhara. Lakini katika siku zijazo, nitawaangalia, ili
niwajenge na kuwapanda—hili ji tangazo la Yahwe. 29 Katika siku hizo hakuna
atakayesema tena, “Baba za watu wamekula zabibu kali, bali meno ya watoto ni
butu.' 30 Kwa maana kila mtu atakuwa katika uovu wake mwenyewe; kila alaye
zabibu kalai, meno yake yataakuwa butu. 31 Angalia, siku zinakuja—hili ni tangazo
la Yahwe—nitakapoanzisha aganao jipya pamaoja na nyumba aya Israeli na nyumba
ya Yuda. 32 Halitakuwa kama agano ambalo nilianzisha na baba zao nilipowatoa
kwa mkono wao nje ya nchi ya Missiri. Hizo zzilikuwa siku ambapo walilivunja
aaganao lanaahu, ingawa nilikuwa mme kwao—hili ni tangazo la Yahwe. 33 Lakaini
hili ni agano nitakaloanzisha na nyumba ya Israeli baada ya siku hizi—hili ni tangazo
la Yahwe: Nitaiweka sheria yangu ndani yao na nitaiandika juu ya mioyo yao,
kwa maana nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watau wangu. 34 Kisha kila mtu
hatamfundisha jiranai yake, wala mtu hatamfundisha ngugu yake akisema, 'Mjue
Yahwe!' Kwa maana wao wote, kuanzia mdogo wao hata mkubwa, watanijua—
hili ni tangazo la Yahwe—kwa maana nitawasamehe uovu wao na sitazikumbuka
tena dhambi zao.”' 35 Yahwe anasema hivi—Yahwe, yeye afanyaye jua kuangaza
mchana na kuzipanga mwezi na nyota kuangaza usiku. Yeye ndiye aiwekaye bahari
katika mwendo ili mawimbi yake yaungurume. Yahwe wa majeshi katika ajina lake.
36 Anasema hivi, ikiwa tu mambo haya ya akudumu yakitoweka machoni panaagu—
hili ni agizo la Yahwe—uzao wa Israeli hawatasimama mbaalai nami wasiwe taiafa.”
37 Yahwe anasema hivi, “Kama tu urefu wa mbingu unaweza kupimwa, na kama tu
misingi ya dunia chini inaweza kugunduliwa, nitawakataa uzao wote wa Israeli kwa
sababu ya yote waliyofanya—hili ni tangazo la Yahwe.” 38 “Angalia, siku zinakuja—
hili ni tanagazo la Yahwe—ambapo mji utajengwa tena kwa ajili yanagu, kutoka
Mnara wa Hananeli hadi kwenye Lango la Pembeni. 39 Kisha mistari ya kupimia
itaenda nje hadi mbali, hadi kwenye kilima cha Garebu na kuzunguka Goa. 40 Bonde
lote la miili iliyokufa na majivu, na shamaba lenye matuta linalofika hadi Bonde la
Kidroni mbali hadi kwenye kona ya Lango la Farasi upande wa mashariki, litateuliwa
kwa ajili ya Yahwe. Mji hautang'olewa wala kupinduliwa tena, milele.”

# 32

1 Neno likaja kwa Yeremia kutoka kwa Yahwe katika mwaka wa kumi wa Sedekia
mfalme wa Yuda, katika mwaka wa kumi na nane wa Nebukadreza. 2 Katika wakati
huo, jeshsi la mfalme wa Babeli lilikuwa limeuzunguka Yerusalemu, na Nehemia
nabii alikuwwa amefungwa katika uwanja wa walinzi katika nyumba ya mfalme
wa Yuda. 3 Sedekia mfalme wa Yuda alikuwa amemfunga na kusema, “Kwa nini
unatabiri na kusema, 'Yahwe anasema hivi: Angalia, niko karibu kuweka mji huu
katika mikono ya mfalme wa Babeli, na atauteka. 4 Sedekia mfalme wa Yuda
hatapona kutoka kwenye mikono ya Wakaldayo, kwa maana hakika atatiwa katika
mkono wa mfalme wa Babeli. Mdomo wake utazumzia kwenye mdomo wa mfalme,
na macho yake yatayaona macho ya mfalme. 5 Atampeleka Sedekia Babeli, na
atabaki huko hadi nimuadhibu—hili ni tangazo la Yahwe. Ingawa unapigana dhidi
ya Wakaldayo, hautafanikiwa.” 6 Yeremia akasema, “Neno la Yahwe likaja kwangu,
likisema, Angalia, Hanameli mwana wa Shalumu mjomba wako anakuja kwako na
atasema, 7 “Linunue shamba langu ambalo liko katika Anathothi kwa ajili yako, kwa
maana haki ya kununua ni yako.”” 8 Kisha, kama Yahwe alivyotangaza, Hanameli,
mwana wa mjomba wangu, akaja kwangu katika uwanja wa walinzi, na akasema
kwangu, 'Linunue shamba langu kwa ajili yako ambalo liko Anathothi katika nchi
ya Benyamini, kwa maana haki ya urithi ni ya kwako, na haki ya kulinunua ni
yako. Linunue kwa ajili yako.' Kisha nilijua kuwa hili lilikuwa neno la Yahwe. 9 Kwa

hiyo nililinua shamba katika Anathothi kutoka kwa Hanameli, mwana wa mjomba
wangu, na nilipima fedha kwa ajili yake, shekeli kumi na saba katika uzito. 10 Kisha
niliandika katika barua na kuitia muhuri, na kulikuwa na mashadi wakaishuhudia.
Kisha nikampa fedha katika mizani. 11 Kisha nikaichukua hati ya manunuzi ambayo
ilikuwa imepigwa muhuri, kwa kuifuata amri na taratibu, na kama ilivyo ada. 12 Ile
barua nikampa Baruku mwana wa Neria wa Maaseya mbele ya Hanameli, mwana
wa mjomba wangu, na mashahidi waliotia sahihi kwenye barua iliyopigwa muhuri,
na mbele ya Wayahudi wote waliokaa katika uwanja wa walinzi. 13 Kwa hiyo
nikampa amri Baruku mbele yao. Nilisema, 14 Yahwe, Mungu wa Israeli, anasema
hivi: Chukua nyaraka hizi, vyote hati hii ya manunuzi iliyopigwa muhuri na nakala
zisizopigwa muhuri za manunuzi, na uziweke katika chungu cha udongo ili vidumu
kwa muda mrefu. 15 Kwa maana Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi:
Nyumba, mashamba, na mashamba ya mizabibu vitanunuliwa tena katika nchi hii.
16 Baada ya kumpa Baruki mwana wa Neria ile hati ya manunuzi, nikaomba kwa
Yahwe nikasema, 17 Ole, Bwana Yahwe! Angalia! Wewe peke yako umezitengeneza
mbingu na dunia kwa nguvu zako kuu na kwa mkono wako ulioinuka. Hakuna kitu
ambacho ukisema kwako ni kigumu sana kukifanya. 18 Wewe huonesha agano la
uaminifu kwa maelfu na kumimina makosa ya wanadamu katika mapaja ya watoto
wao baada yao. Wewe ni Mungu mkuu na mwenye nguvu. 19 Wewe ni mkuu katika
hekima na una nguvu katika matendo, kwa maana macho yako yanaona njia zote za
watu, ili kumlipa kila mtu stahiki ya matendo yake. 20 Ulifanya ishara na maajabu
katika nchi ya Misiri. Hata leo hapa Israeli na kati ya wanadamu wengine wote,
umelifanya jina lako kuwa maarufu. 21 Kwa maana uliwanunua watu wako Israeli
kwa ishira na maajabu, kwa mkono hodari, kwa mkono ulioinuka, na kwa hofu kuu.
22 Kisha uliwapa nchi hii—ambayo uliapa kwa babu zao kwamba utawapa—nchi
itiririkayo maziwa na asali. 23 Hivyo walingia na kuimiliki. Lakini hawakuitii sauti
yako wala kuishi kwa kuitii sheria yako. Hawakufanya chochote ulichowaamuru
kufanya, kwa hiyo umeleta juu yao majanga haya yote. 24 Angalia! Urefu wa
maboma haya umefika hadi kwenye mji ili kuuteka. Kwa sababu ya upanga, njaa, na
tauni, mji umetiwa kwenye mikono ya Wakaldayo wanaopigana dhidi yake. Kwa
maana ulichosema kitatokea sasa kinatokea, na ona, unatazama. 25 Kisha wewe
mwenyewe uliniambia, “Nunua shamba kwa fedha kwa ajili yako na mashahidi
wameshuhudia, ingawa mji huu unatiwa mikononi mwa Wakaldayo.”” 26 Neno
la Mungu likaja kwa Yeremia, likisema, 27 “Angalia! Mimi ni Yahwe, Mungu wa
wanadamu wote. Kuna kitu cho chote kigumu sana kwangu kukifanya? 28 Kwa hiyo
Yahwe anasema hivi, 'Ona, niko karibu kuutia mji huu kwenye mikono ya Wakaldayo
na Nebukadreza, mfalme wa Babeli. Atauteka. 29 Wakaldayo wanaopigana dhidi
ya mji huu watakuja na kuwasha moto kwenye mji huu na kuunguza, pamoja na
nyumba juu ya paa la watu waliomwabudu Baali na kumimina dhabihu kwa miungu
wengine ili kunikasirisha. 30 Kwa maana watu wa Israeli na Yuda hakika wamekuwa
watu wanaofanya maovu mbele ya macho yangu tangu ujana wao. Watu wa Israeli
hakika wameniudhi kwa matendo ya mikono yao—hili ni tangazo la Yahwe. 31 Yahwe
anatangaza kwamba mji huu umekuwa sababu ya hasira yangu na ghadhabu yangu
tangu siku walipoujenga. Umekuwa hivyo hata leo. Kwa hiyo nitaundoa mbele ya uso
wangu 32 kwa sababu ya uovu wote wa watu wa Israeli na Yuda, mambo waliyofanya
ili kunichukiza—wao, wafalme wao, wana wa wafalme, makuhani, manabii, na kila
mtu katika Yuda na wakaaji wa Yerusalemu. 33 Wamenigeuzia migongo yao badala
ya nyuso zao, ingawa niliwafundisha kwa furaha. Nilijitahidi kuwafundisha, lakini
hakuna hata mmoja wao aliyenisikiliza ili kupokea marekebisho. 34 Walisimamisha
sanamu zao za ajabu katika nyumba inayoitwa kwa jina langu, ili kunitia unajisi.

[35] Wakazijenga sehemu za juu katika Bonde la Beni Hinomu ili kuwatia katika moto
wana wao na binti zao kwa ajili ya Moleki. Mimi sikuwaagiza. Sikuweka akilini
mwangu kamwe kwamba watafanya mambo maovu na kwa hiyo kuwasabisha Yuda
watende dhambi. [36] Kwa hiyo sasa, Mimi, Yahwe, Mungu wa Israeli, kuhusu mji huu
ninasema hivi, 'mji ambao mnasema, 'Umetiwa mikononi mwa mfalme wa Babeli
kwa upanga, njaa, na pigo.' [37] Ona, niko karibu kuwakusanya kutoka kila nchi
nilikowapeleka katika hasira yangu, ghadhabu, hasira kuu. Niko karibu kuwarudisha
kwenye sehemu hii na kuwawezesha kuishi katika usalama. [38] Kisha watakuwa
watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao. [39] Nitawapa moyo mmjoa na na njia
moja ya kuniheshimu kila siku ili kwamba yawepo mema kwa ajili yao na uzao
wao baada yao. [40] Kisha nitafanya pamoja nao agano la milele, ili nisiache kufanya
mema kwa ajili yao. nitajiwekea heshima katika mioyo yao, ili kwamba wasiniache.
[41] Kisha nitajifurahisha katika kufanya mema kwao. Kwa uaminifu nitawapanda
katika anchi hii kwa moyo wangu wote na maisha yangu yoye. [42] Kwa amaana
Yahwe anasema hivi, 'Kama tu nilivyoyaleta majanga haya makubwa yote juu ya
watu hawa, hivyo hivyo nitaleta juu yao mambo mema niliyosema kwamba nitafanya
kwa ajili yao. [43] Basi mashamba yatanunuliwa katika nchi hii, ambayo mnaisema,
“Hii ni nchi iliyoharibiwa, isiyo na mwanadamu wala mnyama. Imetiwa mikononi
mwa Wakaldayo” [44] Watanunua mashamba kwa fedha na kuandika katika barua
zilizopigwa muhuri. Watawakusanya mashahidi katika nchi ya Benyamini, wote
kuzunguka Yerusalemu na miji ya Yuda katika miji ya nchi yenye vilima, na katika
nchi tambarare, na katika miji ya Negebu. Kwa maana nitawarejesha wafungwa
wao—hili ni tangazo la Yahwe.”'

# 33

[1] Kisha neno la Yahwe likaja kwa Yeremia mara ya pili, alipokuwa bado amefungwa
ndani ya uwanja wa walinzi, likisema, [2] Yahwe muumbaji, anasema hivi—Yahwe,
aumbaye ili athibitishishe—Yahwe ndilo jina lake, [3] 'Niite, na nitakuitika, nitakuelezea
mambo makuu, siri ambazo huzielewi.' [4] Kwa maana Yahwe, Mungu wa Israel,
anasema hivi kuhusu nyumba zilizo katika mji huu na nyumba za wafalme wa
Yuda zilizobomolewa kwa sababu ya maboma na upanga, [5] Wakaldayao wanakuja
kupigana na kuzijaza nyumba kwa hizi kwa majeshi ya watu ambao wataua katika
hasira yangu na ghadhabu yangu, nitakapouficha mji huu uso wangu kwa sababu
ya uovu wao wote. [6] Lakini ona, niko karibu kuleta uponyaji na tiba, kwa
maana nitawaponya na nitawapa wingi wa, amani na uamainifu. [7] Kwa maana
nitawarudhisha wafungwa wao wa Yuda na Israeli; nitawajenga tena kama ilivyokuw
mwanzo. [8] Kisha nitawatakasa uovu wote walioufanya dhidi yangu. Nitasamehe
makosa yote waliyonitenda, na na njia zote walizo asi dhidi yangu. [9] Kwa maana
mji huu kwa ajili yangu utakuwa chombo cha furaha, nyimbo, sifa na heshima
kwa mataiafa yote ya dunia ambao watasikia mambo yote mema ninayokwenda
kufanya kwa ajili ya huu mji. Kisha wataogopa na kutetemeka kwa sababu ya
mambo yote mema na amani nitayoupa mji huu.' [10] Yahwe anasema hivi, 'Katika
sehemu hii ambayo sasa mnaisema, “Imetengwa, sehemu isiyo na mwanadamu
wala mnyama,” katika mji huu wa Yuda, na katika mitaa ya Yerusalemu ambayo
imetengwa bila mwanadamu wala mnyama, zitasikika tena [11] sauti za furaha na
sauti za shangwe, sauti ya bwana arusi na sauti ya bibi arusi, sauti za wale wasemao,
wanapoleta shukrani katika nyumba ya Yahwe, “Mshukuruni Yahwe wa majeshi,
kwa maana Yahwe ni mwema, na upendo wake usioshindwa wadumu milele!” Kwa
maana nitawafanaya tena wafungwa wa nchi kuwa walivyokuwa mwanzo,' asema
Yahwe. [12] Yahwe wa majeshi asema hivi: Katika sehemu hii ya ukiwa, ambamo

sasa hakuna mwanadamu wala mnyama—katika miji yake yote kutakuwepo tena
malisho ambapo wachungaji wataweza kupumzisha makundi yao. [13] Katika miji
hii katika nchi ya vilima, nchi tambarare, na Negevu katika nchi ya Benyamini na
kuzunguka Yerusalemu yote, na katika miji ya Yuda, makundi yatapata njia chini
ya mkono wa yule anayewahesabu,' asema Yahwe. [14] Angalia! Siku zinakuja—
hili ni tangazo la Yahwe—ambapo nitafanya niliyoahidi kwa nyumba ya Israeli na
nyumba ya Yuda. [15] Katika siku hizo na katika wakati huo nitachipua shina la haki
kwa ajili ya Daudi, na litafanaya hukumu na haki katika nchi. [16] Katika siku hizo
Yuda wataokolewa, na Yurusalemu utaishi katika usalama, kwa maana hivi ndivyo
atakavyoitwa, “Yahwe ni haki ni haki yetu.” [17] Kwa maana Yahwe anasema hivi:
'Mwana kutoka ukoo wa Daudi hatakosa kuketi katika kiti cha nyumba ya Israeli,
[18] wala mtu kutoka ukuhani wa Kilawi hatakosa kutoa sadaka za kuteketezwa mbele
zangu, kutoa sadaka za chakula, na kutoa sadaka za nafaka wakati wote.”' [19] Neno
la Yahwe likaja kwa Yeremia, likisema, [20] “Yahwe anasema hivi: 'Kama mkiweza
kulivunja agano langu la mchana na usiku ili kwamba siku isikawie wala usiku
usikawie kuja kwa wakati wake, [21] basi mtaweza u kulivunja agano langu na Daudi
mtumishi wangu, ili kwamba aspate mwana wa kuketi juu ya kiti chake cha enzi,
na gano langu na makuhuni wa Kilawi, watumishsi wangu. [22] Kama vile majeshsi
ya mbinguni yasivyoweza kuhesabika, na kama vile mchanga wa ufukwe wa bahari
usivyoweza kupimwa, ndivyo nitakavyouongeza uzao wa Daudi mtumishi wangu na
Walawi watumikao mbele zangu.” [23] Neno la Mungu likaja kwa Yeremia, likisema,
[24] Hamkuzingatia walichotangaza watu hawa waliposema, 'Zile Familia mbili ambazo
Yahwe alizichagua, sasa amezikataa'? Kwa jinsi hii hii waliwapuuza watu wangu,
wakisema kwamba si taifa tena katika macho yao. [25] Mimi, Yahwe, nasema hivi,
'Kama sijalithibitisha agano la mchana na usiku, na kama sijaziweka sheria za
mbingu na dunia, [26] basi nitawakataa uzao wa Yakobo na Daudi mtumishi wangu,
na nisilete mtu kutoka kati yao wa kutawala juu ya uzao wa Abrahamu, Isaka, na
Yakobo. Kwa maana nitawarudisha wafubgwa wao na kuonesha huruma kwao.”'

# 34

[1] Neno lililomjia Yeremia kutoka kwa Yahwe, wakati Nebukadreza mfalme wa
Babeli, majeshi yake yote, pamoja na falme zote za dunia, maeneo yote yaliyo chini ya
mamlaka yake, na watu wake wote walikuwa wanapigana vita dhidi ya Yerusalemu
na miji yake yote, kusema: [2] 'Yahwe, Mungu wa Israeli, anasema hivi: Nenda na
uzungumze kwa Sedekia mfalme wa Yuda na useme kwake, 'Yahwe asema hivi:
Angalia, niko karibu kuutia mji huu mkononi mwa mfalme wa Babeli. Atauchoma
moto. [3] Hautapona kutoka mkono wake, kwa maana kwa hakika utakamatwa na
kutiwa mkononi mwake. Macho yako yatayaangalia macho ya mfalme wa Babeli;
atazungumza kwako moja kwa moja ukiwa unaenda Babeli.' [4] Sedekia mfalme wa
Yuda, sikiliza neno la Yahwe! Yahwe anasema hivi kuhusu wewe, 'Hautakufa kwa
upanga. [5] Utakufa katika amani. Kama kwenye mafukizo ya babu zako, wafalme
waliokuwepo kabla yako, watauchoma mwili wako. Watasema, 'Ole, bwana!”
Watakuomboleza. Sasa nimesema—hili ni tangazo la Yahwe.” [6] Kwa hiyo Yeremia
nabii akatangaza kwa Sedekia mfalme wa Yuda maneno haya yote katika Yerusalemu.
[7] Jeshi la mfalme wa Babeli likafanya dhidi ya Yerusalemu na miji yote ya Yuda
iliyobaki: Lakishi, na Azeka. Miji hii ya yuda ilisalia kama miji yenye maboma.
[8] Neno lilomjia Yeremia kutoka kwa Yahwe baada ya mfalme Sedekia kufanya agano
na watu wote katika Yurusalemu, ili kuwatanagazia uhuru [9] ya kwamba kila mtu
lazima amwachie huru mtumwa wake wa Kiebrania, wote wa kiume na wa kike, kwa
hiyo mtu alipaswa kutomtumikisha Myahudi, ambaye alikuwa ndugu yake. [10] Kwa

hiyo watu wote na viongozi wakaingia katika agano kwamba kila mtu amwachie huru
mtumwa wake wa kiume na waikke ili asiwe mtumwa tena. Walitii na kuwaweka
huru. [11] Lakini baada ya hapo walibadili akili zao. Wakawarudisha watumwa ambao
walikuwa wamewaachia huru. Wakawalazimisha kuwa wataumwa tena. [12] Kwa hiyo
neno la Yahwe likaja kwa Yeremia, likisema, [13] "Yahwe, Mungu wa Israeli, anasema
hivi, 'Mimi mwenyewe nilifanya agano na babu zenu katika siku ambayo niliwatoa
nje ya nchi ya Misiri, nje ya nyumba ya utumwa. Hapo ndipo niliposema, [14] Katika
mwisho wa mwaka wa saba, kila mtu lazima amwachie ndugu yake, Mwebrania
mwenzake aliyejiuza mwenyewe kwako ili kukutumikia kwa miaka sita. Mwagize
aende kwa uhuru." Lakini babu zenu hawakunisikiliza wala kutega masikio yao
kwangu. [15] Sasa ninyi wenyewe mlitubu na kuanza yaliyomema katika macho yangu.
Mlitangaza uhuru, kila mtu kwa jirani yake, na mlifanya agano mbele zangu kwenye
nyumba iitwayo kwa jina langu. [16] Lakini tena mmegeuka na kulichafua jina langu;
mmemsababisha kila mtu kumleta tena mtumwa wake wa kiume na wa kike, wale
mliowachie kwenda walikotaka. Mmewalazimisha kuwa watumwa tena.' [17] Kwa hiyo
Yahwe asema hivi, 'Ninyi wenyewe hamkunisikiliza. Mlipaswa kuwa mmetangaza
uhuru, kila mmoja wenu, kwa ndugu zenu na Waisraeli wenzenu. Kwa hiyo angalia!
Niko karibu kutangaza uhuru kwenu—hili ni tangazo la Yahwe—uhuru wa upanga,
tauni, na njaa, kwa maana naenda kuwafanya kitu cha ajabu katika macho aya kila
ufalme juu ya dunia. [18] Kisha nitashughulika na watu waliolivuja agano langu, ambao
hawakuyashika maneno ya agano ambalo walilithibitisha mbele zangu walipomkata
ng'ombe dume katika vipande viwili na kutembea katika vipande vyake, [19] na kisha
viongozi wa Yuda na Yerusalemu, matowashi na makuhani, na watu wote wa nchi
wakatembea katika vipande vya yule ng'ombe dume. [20] Nitawatia katika mikono
ya adui zao na katika mikono ya hao wanaoutafuta uhai wao. Miili yao itakuwa
chakula cha ndege wa angani na wanyama juu ya dunia. [21] Kwa hiyo nitawatia
Sedekia mfalme wa Yuda na viongozi wake kwenye mikono ya adui zao na kwenye
miko ya wale wanaoutafuta uhai wao na katika mikono ya majeshi ya mfalme wa
Babeli ambayo yameinuka dhidi yenu. [22] Angalia, niko karibu kutoa amari—hili ni
tangazo la Yahwe—na nitawaleta tena kwenye mji huu ili wapigane dhidi yake, na
kuunguza kwa moto. Kwa maana nitaigeuza miji ya Yuda kuwa sehemu za ukiwa
ambamo hapatakuwa na wakaaji."

# 35

[1] Neno kutoka kwa Yahwe likamjia Yeremia katika siku za Yehoyakimu mwana
wa Yosia mfalme wa Yuda, kusema, [2] "Nenda kwenye familia ya Warekabi na
zungumza nao. Kisha uwalete kwenye nyumba yangu, mle ndani ya moyawapo
ya vyumba, na uwape divai wanywe." [3] Hivyo nilimchukua Yaazania mwana wa
Yeremia mwana wa Habasinia na ndugu zake, wanawe wote, na familia yote ya
Warekabi. [4] Nikawapeleka wote kwenye nyumba ya Yahwe, katika vyumba vya wana
wa Hanani mwana wa Igdalia, mtu wa Mungu. Vyumba hivi vilikuwa karibu na
chumba cha viongozi, ambacho kilikuwa juu ya chumba cha Maaseya mwana wa
Shalumu, mtunza lango. [5] Kisha nikaleta mabakuli na vikombe vilivyojaa divai mbele
ya Warekabi na kusema kwao, 'Kunyeni divai." [6] Lakini walisema, "hatutakunywa
divai yoyote, kwa maana babu yetu, Yonadabu mwana wa Rekabu, alituamuru,
Msinywe divai yoyote, ninyi wala uzao wenu, milele. [7] Pia, msijenge nyumba yoyote,
kupanda mbegu zozote, wala kupanda shamba lolote la mizabibu; hivi siyo kwa ajili
yenu. Kwa maana lazima muishi katika hema maisha yenu yote, ili kwamba muweze
kuishsi siku nyingi katika nchi mnayoishi kama wageni.' [8] Tumeitii sauti ya Yonadabu
mwana wa Rekabu, babu yetu, katika yote aliyotuamuru, kutokunywa divai maisha

yetu yote, sisi, wake zetu, wana wetu, na binti zetu. 9 Hatutajenga nyumba kwa ajili ya
kuishi ndani, na hatutakuwa na shamba la mizabu, konde, wala mbegu ya kumiliki
sisi. 10 Tumeishi katika hema na tumetii na kufanya yote aliyotuamuru Yonadabu
babu yetu. 11 Lakini Nebukadreza mfalme wa Babeli alipoivamia nchi, tulisema,
'Njoo, lazima twende Yerusalemu ili tupone na mkono wa Wakaldayo na majeshi
ya Waaramu. 'Kwa hiyo tunaishi Yerusalemu." 12 Kisha neno la Yahwe likaja kwa
Yeremia, likisema, 13 "Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli, anasema hivi, 'Nenda na
useme kwa wanaume wa Yuda na wakaaji wa Yeruslemu, 'Hamtapokea maelekezo na
kulisikiliza neno langu? —hili ni tangazo la Yahwe. 14 Maneno ya Yonadabu mwana
wa Rekabu aliyowapa wanawe kama amri. wasinywe divai yoyote, yameheshimiwa
hadi leo. Wameitii amri ya babu yao. Lakini mimi, nimekuwa nikifanya matangazo
kwenu bila kukoma, lakini hamnisikilizi. 15 Niliwatuma kwenu watumishi wangu
wote, manabii, nilikuwa nawatuma bila kukom ili waseme, 'Kila mtu auache uovu
wake na kutenda matendo mema; asiwepo mtu wa kuifuata miungu mingine tena
na kuiabudu. Bdala yake, rudini kwenye nchi niliyowapa ninyi na babu zenu,' bado
hamtanisikiliza wala kutega maskio yenu kwangu. 16 Kwa maana uzao wa Yonadabu
mwana wa Rekabu wamezishika amri za babu yao alizowapa, lakini watu hawa
hupuuza kunisikiliza." 17 Kwa hiyo Yahwe, Mungu wa majeshi na Mungu wa Israeli,
asema hivi, 'Angalia, Ninaleta juu ya Yuda na juu ya kila mtu anayeishi Yerusalemu,
majanga yote niyotamka dhidi yao kwa sababu niliwaambia, lakini hawakusikiliza;
niliwaita, lakini hawakuitika." 18 Yeremia akasema kwa familia ya Warekabi, "Yahwe
wa majeshi, Mungu wa Israeli asema hivi: mmezisikiliza amri za Yonadabu babu
yenu na kuzishika zote—mmeyatii yote aliyowaamuru kufanya— 19 kwa hiyo Yahwe
wa majeshi, Mungu wa Israeli, asema hivi, 'Siku zote kutakuwa na mtu kutoka uzao
wa Yonadabu mwana wa Rekabu kwa ajili ya kunitumikia."'

# 36

1 Ilikuja tokea katika mwaka wa nne wa Yehoyakimu mwana wa Yosiah mfalme
wa Yuda, kwamba neno hili lilikuja kwa Yeremiah kutoka kwa Yahwe, na alisema,
2 "Chukua kitabu kwa ajili yako na uandike juu yake maneno yote ambayo
nimekwisha kukuambia kuhusiana na Israel na Yuda, na kila taifa. Fanya hivi
kwa kila kitu nilichokuambia tokea siku za Yosia mpaka siku ile. 3 Huenda watu
wa Yuda watasikiliza majanga yote ambayo ninakusudia kuleta juu yao. Huenda
kila mmoja ataacha njia zake mbaya, ili kwamba niweze kuwasamehe maovu yao
na dhambi zao." 4 Kisha Yeremia alimwita Baruku mwana wa Neria, na Baruku
aliandika kwenye kitabu, kwa imla ya Yeremia, maneno yote ya Yahwe yalizunguzwa
kwake. 5 Kisha Yeremia alitoa amri kwa Baruku. Alisema, "Niko gerezani na siwezi
kwenda kwenye nyumba ya Yahwe. 6 Kwa hiyo unapaswa uende na kusoma kutoka
kwenye kitabu ulichoandika kwa imla yangu. Kwa siku ya kufunga, unapaswa usome
maneno ya Yahwe kwenye masikio ya watu katika nyumba yake, na pia kwenye
masikio ya Yuda yote waliokuja kutoka katika miji yao. Tangaza maneno haya kwao.
7 Huenda maombi yao ya rehema yatakuja mbele ya Yahwe. Huenda kila mtu ataacha
njia mbaya, kwani gathabu na hasira ya Yahwe imetangazwa dhidi ya watu kwa
ukali." 8 Kwa hiyo Baruku mwana wa Neria alifanya kila kitu ambacho Yeremia
nabii alimwamuru yeye kufanya. Alisoma kwa sauti maneno ya Yahwe ndani mwa
nyumba ya Yahwe. 9 Ilikuja tokea katika mwaka wa tano na mwezi wa tisa kwa
Yehoyakimu mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda, kwamba watu wote Yerusalemu na
watu waliotoka Yerusalemu toka miji ya Yuda walitangaza kufunga kwa kumheshimu
Yahwe. 10 Baruku alisoma kwa sauti maneno ya Yeremia katika nyumba ya Yahwe,
kutoka kwenye chumba cha Gamaria mwana wa Shafani mwandishi, katika ua wa

juu, kwa mlango wa kuingilia wa nyumba ya Yahwe. Alifanya hivi kwa masikio
ya watu wote. 11 Basi Mikaya mwana wa Gemaria alisikia maneno yote ya Yahwe
kwenye kitabu. 12 Alienda chini kwenye nyumba ya mfalme, kwenye chumba cha
katibu. Tazama, maafisa wote walikuwa wamekaa hapo: Elishama mwandishi,
Delaiah mwana wa Shemaiah, Elnathan mwana wa Achbor, Gemaria mwana wa
Shefani, na Sedekia mwana wa Hananiah, na maafisa wote. 13 Kisha Mikaya alitoa
taarifa ya maneno yote kwao ambayo alikuwa amesikia ambayo Baruku alisoma
kwa sauti kwenye masikio ya watu. 14 Kwa hiyo maafisa wote walimtuma Jehudi
mwana wa Nethania mwana wa Shelemiah mwana wa Kushi, kwa Baruku. Jehudi
alisema kwa Baruku, “Chukua kitabu katika mkono wako, kitabu ambacho ulikuwa
unakisoma kwa masikio ya watu and kuja.” Kwa hiyo Baruku mwana wa Neria
alichukua kitabu katika mkono wake na alienda kwa maafisa. 15 Kisha walisema
naye,”Kaa chini na usome haya katika masikio yetu.” Kwa hiyo Baruku akasoma
kitabu. 16 Ilitokea wakati waliposikia haya maneno yote, kila mtu alipatwa na hofu
kwa mtu aliye karibu naye na kusema kwa Baruku, “Kwa hakika tunapaswa kutoa
taarifa ya maneno haya yote kwa mfalme.” 17 Kisha walimuuliza Baruku, “Tuambie,
ulipataje kuandika maneno yote haya kwa imla ya Yeremia?” 18 Baruku aliwaambia,
“Alitoa imla ya maneno haya yote kwangu, na nikayaandika kwa wino kwenye
kitabu hiki.” 19 Kisha maafisa walisema kwa Baruku, “Nenda, jifiche mwenyewe,
na Yeremiah, pia. Usipatikane mtu yeyote kujua uko wapi.” 20 Kisha walienda kwa
uwanja wa mfalme na wakatoa taarifa ya maneno haya kwake. Lakini kwanza
walikihifadhi kitabu kwenye chumba cha katibu Elishama. 21 Basi mfalme alimtuma
Yehudi kuchukua kitabu. Yehudi alikichukua toka chumba cha Elishama katibu.
Kisha alikisoma kwa sauti kwa mfalme na wote maafisa walikuwa wamesimama
karibu naye. 22 Sasa mfalme alikuwa amesimama kwenye nyumba ya majira ya
baridi katika mwezi wa tisa, na mkaa ulikuwa unawaka mbele yake. 23 Ilitokea
wakati Yehudi aliposoma kurusa tatu au nne, mfalme angeweza kuikata kwa kisu
na kuitupa kwenye moto katika mkaa mpaka kitabu chote kiliteketea. 24 Lakini wala
mfalme wala yeyote wa mjakazi wake aliyesikia haya maneno yote aliogopa, wala
hawakuchana nguo zao. 25 Elnathani, Delaya, na Gemaria walikuwa wamemuomba
mfalme asikichome kitabu, lakini hakuwasikiliza. 26 Basi mfalme alimwamuru
Yerameeli, ndugu, Seraya mwana wa Azrieli, na Shelemia mwana wa Abdeeli
kumfunga Baruku mwandishi na Yeremia nabii, lakini Yahwe alikuwa amewaficha.
27 Kisha neno la Yahwe lilikuja kwa Yeremia baada ya mfalme kuwa amechoma
kitabu na maneno ya Baruku yaliyokuwa yameandikwa kwa imla ya Yeremia, na
alisema, 28 “Rudi, chukua kitabu kingine kwa ajili yako, na uandike maneno haya yote
ambayo yalikuwa kwenye kitabu cha kwanza, ambacho Yehoyakimu mfalme wa Yuda
alikichoma. 29 Kisha unapaswa kusema hivi kwa mfalme Yehoyakimu mfalme wa
Yuda: 'Ulichoma hicho kitabu! Na ulisema: Kwanini umeandika juu yake, “ Mfalme
wa Babeli hakika atakuja na kuharibu nchi hii, kwa kuwa atawaangamiza wanaume
wote na wanyama ndani yake?” 30 Kwa hiyo Yahwe anasema hivi kuhusu wewe,
Yehoyakimu mfalme wa Yuda: “Hakuna mzao wako atawahi kukaa kwenye kiti cha
Daudi. Kama wewe, maiti yako itatupwa kwenye siku ya joto na usiku wa baridi.
31 Kwa kuwa nitakuadhibu, wazao wako, na wajakazi wako kwa maovu yenu yote.
Nitaleta kwenu, kwa wakazi wote wa Yerusalemu, na kwa kila mtu Yuda majanga
ambayo nimewatishia ninyi, lakini kwa hamkuwa makini.” 32 Kwa hiyo Yeremia
alichukua kitabu kingine na akampa Baruku mwana wa Neria mwandishi. Baruku
aliandika juu yake kwa imla ya Yeremia maneno yote ambayo yalikuwa katika kitabu
kilichochomwa moto na mfalme Yehoyakimu mfalme wa Yuda. Zaidi, maneno mengi
ya kufanana yaliongezwa kwenye kitabu hiki.

# 37

1 Sasa Sedekia mwana wa Yosia alitawala kama mfalme badala ya Yehoyachin
mwana wa Yehoyakimu. Nebukadreza mfalme wa Babeli alikuwa amemfanya
Sedekia mfalme juu ya nchi ya Yuda. 2 Lakini Sedekia, wajakazi wake, na watu wa
nchi hawakusikiliza maneno ya Yahwe ambayo alitangaza kwa mkono wa Yeremia
nabii. 3 Kwa hiyo Mfalme Sedekia, Yehukali mwana wa Shelemia, na Zefania mwana
wa Maaseia kuhani alituma ujumbe kwa Yeremia nabii. Walisema, “Omba kwa niaba
kwa Yahwe Mungu wetu.” 4 Sasa Yeremia alikuwa anakuja na kwenda miongoni
mwa watu, kwa kuwa alikuwa bado hajawekwa ndani ya gereza. 5 Jeshi la Farao
lilitoka Misri, na Wakaldayo waliozingira Yerusalem walisikia habari kuhusu wao
na kuondoka Yerusalem. 6 Kisha neno la Yahwe lilikuja kwa Yeremia nabii na
kusema, 7 “Yahwe, Mungu wa Israel, asema hivi: Hiki ndivyo utakavyosema kwa
mfalme wa Yuda, kwa sababu amekutuma wewe kutafuta ushauri toka kwangu,
'Ona, jeshi la Farao, ambalo lilikuja kukusaidia, liko tayari kurudi Misri, kwenye nchi
yao. 8 Wakaldayo watarudi. Watapigana dhidi ya mji huu, kuuteka, na kuuchoma.'
9 Yahwe asema hivi: Msidaganyane kwa kusema, “Hakika Wakaldayo wanatuacha
sisi,' kwa kuwa hawatatuacha. 10 Hata kama mmelishinda jeshi la Wakaldayo lote
ambalo linapigana nanyi ili kwamba wanaume waliojeruhiwa walibakizwa katika
mahema yao, wangeweza kunyanyuka na kuchoma mji huu.” 11 Basi ilikuwa wakati
jeshi la Wakaldayo lilipoondoka Yerusalem wakati jeshi la Farao lilikuwa linakuja,
12 kisha Yeremia aliendа toka Yerusalem kwenda nchi ya Benjamini. Alitaka kumiliki
njia ya nchi huko miongoni mwa watu wake. 13 Kama alivyokuwa katika mlango
wa Benjamini, mlinzi mkuu aliyekuwa hapo. Jina lake lilikuwa Yeria mwana wa
Shelemia mwana wa Hanania. Alimshika kwa kumnyakua Yeremia nabii na kusema,
“ Mnatoka jangwani kwa Wakaldayo.” 14 Lakini Yeremia alisema, “Hiyo si kweli.
Siendi jangwani kwa Wakaldayo.” Lakini Yeria hakumsikiliza. Alimchukua Yeremia
na kumleta kwa maafisa. 15 Maafisa walikuwa wamemkasirikia Yeremia. Walimpiga
na kumweka gerezani, ambayo ilikuwa nyumba ya Yonathani mwandishi, kwa kuwa
waligeuza kuwa gereza. 16 Kwa hiyo Yeremia alikuwa amewekwa kwenye kifungo
cha chini, ambako alikuwa huko kwa siku nyingi. 17 Kisha mfalme Sedekia alimtuma
mtu mmoja aliyemleta kwenye ikulu. Kwenye nyumba yake, mfalme alimuuliza
binafsi, “Kuna neno: Utatiwa kwenye mkono wa mfalme wa Babeli.” 18 Kisha Yeremia
alisema kwa mfalme Sedekia, “Kwa namna gani nimekutenda dhambi, mjakazi wako,
au watu hawa kwamba umeniweke mimi kwenye gereza? 19 Wako wapi nabii wako,
wale waliotabiri kwa ajili yako na kusema mfalme wa Babeli hatakuja dhidi yako au
dhidi ya nchi hii? 20 Lakini sasa sikiliza, bwana wangu mfalme! Acha ombi langu liwe
mbele yako. Usinirudie mimi kwenye nyumba ya Yonathani mwandishi, au nitakufa
huko.” 21 Kwa hiyo mfalme Sedekia alitoa amri. Wajakazi wake walimwekea mipaka
Yeremia katika uwanja wa walinzi. Alipewa mkate kila siku kutoka mtaa wa waokaji
mkate, mpaka mkate wote mjini uliisha. Basi Yeremia alibaki kwenye uwanja walinzi.

# 38

1 Shefatia mwana wa Matani, Gedalia mwana wa Pashuri, na Pashuri mwana
wa Malkiya alisikia maneno ambayo Yeremia alikuwa akitanganza kwa wato wote.
Alikuwa akisema, 2 “Yahwe asema hivi: Yeyote anayeishi kwenye mji huu atauwawa
kwa upanga, njaa, na pigo. Lakini yeyote ambaye aendae kwa Wakaldayo ataishi.
Atatoroka pamoja na maisha yake mwenyewe, na kuishi. 3 Yahwe asema hivi: Huu
mji huu utapewa kwa mkono wa jeshi la mfalme wa Babeli, na ataukamata.” 4 Kwa
hiyo maafisa walisema kwa mfalme, “Acha mtu huu afe, kwa kuwa kwa njia hii
anadhofisha mikono ya wanaume wapiganaji waliobaki kwenye mji huu, na mikono

ya watu wote. Anatanganza maneno haya, kwa kuwa huyu mtu hafanyi kwa usalama
wa watu hawa, lakini kwa majanga." 5 Basi mfalme Sedekia alisema, "Tazama,
yuko mkononi mwako kwa kuwa hakuna mfalme awezae kumpinga." 6 Kisha
walimchukua Yeremia na kumtupa kwenye kisima cha Malkiya, mwana wa mfalme.
Kisima kilikuwa kwenye uwanja wa mlinzi. Walimshusha Yeremia chini kwa kamba.
Hapakuwa na maji kwenye kisima, lakini kulikuwa na matope, na alizama chini ya
matope. 7 Sasa Ebed Meleki Mkushi alikuwa mmoja wa watowashi katika nyumba ya
mfalme. Alisikia kwamba walikuwa wamemuweka Yeremia kwenye kisima. Sasa
mfalme alikuwa ameketi kwa mlango wa Benjamini. 8 Basi Ebed Meleki aliend
toka nyumba ya mfalme na kuzungumza na mfalme. 9 Alisema, "Bwana wangu
mfalme, hawa wanaume wamefanya uovu kwa namna walivyomtendea Yeremia
nabii. Walimtupa kwenye kisima kwa ajili ya kufa kutokana na njaa, tangu hakuna
chakula zaidi katika mji." 10 Kisha mfalme alitoa amri kwa Ebed Meleki Mkushi.
Alisema, "Chukua amri ya watu thelasini kutoka hapa na mtoe Yeremia nabii nje ya
kisima kabla hajafa." 11 Basi Ebed Meleki alichukua amri ya watu hao na akaenda
nyumba ya mfalme, kwenye ghala la nguo chini ya nyumba. Toka hapo alichukua
vitambaa na nguo zilizochanika na kuyashusha chini kwa kamba kwa Yeremia ndani
ya kisima. 12 Ebed Meleki Mkushi alisema kwa Yeremia, "Weka matambara na
nguo zilizoraruka chini ya mikono yako na juu ya kamba." Basi Yeremia alifanya
hivyo. 13 Kisha walimvuta Yeremia kwa kamba. Kwa njia hii walimtoa kutoka
kisimani. Basi Yeremia alibaki kwenye uwanja wa mlinzi. 14 Kisha Mfalme Sedekia
alituma neno na kumleta Yeremia nabii kwake, kwenye lango la tatu la nyumba
ya Yahwe. Mfalme alisema kwa Yeremia, "Nataka nikuulize kitu. Usinizuilie
jibu mimi." 15 Yeremia alisema kwa Sedekia, "Kama nakujibu, hautaniuawa kwa
hakika? Na kama nakupa ushauri, hautanisikiliza mimi." 16 Lakini Mfalme Sedekia
aliapa kwa Yeremia kwa siri na kusema, "Kama Yahwe aishivyo, yeye aliyetufanya
sisi, Sitakuuwa au kukuweka kwenye mkono wa watu wale wanaotafuta maisha
yako." 17 Kwa hiyo Yeremia alisema kwa Sedekia, "Yahwe, Mungu wa majeshi,
Mungu wa Israel, asema hivi: Kama kwa kweli utatoka kwenda kwa maafisa wa
mfalme wa Babeli basi utaishi, and mji huu hautachomwa. Wewe na familia yako
mtaishi. 18 Lakini kama hautaenda kwa maafisa wa mfalme wa Babeli, basi mji
huu utachukuliwa kwa mkono wa Wakaldayo. Watauchoma, na hautakwepa kutoka
mkono wao." 19 Mfalme Sedekia alisema kwa Yeremia, "Lakini ninaogopa watu
wa Yuda waliotoka jangwani kwenda kwa Wakaldayo, kwa sababu nitapewa katika
mkono wao, kwa kunifanyia vibaya." 20 Yeremia alisema, "Hawatakutoa kwao. Tii
ujumbe toka kwa Yahwe ambao ninakuambia, ili kusudi mambo yataenda vizuri
kwako, na ili kusudi utaishi. 21 Lakini kama unakataa kutoka, hivi ndivyo Yahwe
amenionesha mimi. 22 Tazama! Wanawake wote walioachwa kwenye nyumba yako,
mfalme wa Yuda, ataletwa kwa maafisa wa mfalme wa Babeli. Hawa wanawake
watasema kwako, "Umedaganywa na rafiki zako; wamekuharibu. Miguu yako sasa
imezama kwenye matope, na rafiki zako watakimbia.' 23 Kwa kuwa wake zenu wote
na watoto wataletwa kwa Wakaldayo, na wewe mwenyewe hautatoroka nchi yao.
Utashikwa na mkono wa mfalme wa Babeli, na mji huu utachomwa." 24 Kisha Sedekia
alisema kwa Yeremia, "Usimjulishe yeyote kuhusu maneno haya, ili kwamba usije
kufa. 25 Kama maafisa wanasikia kwamba nimeongea na wewe- kama wanakuja
na kusema kwako, 'Tuambia umezungumza nini pamoja na mfalme. Usitufiche, au
tutakuuwa. Na tuambie nini mfalme amesema kwako'- 26 kisha unapaswa kusema
nao, "Nilishawishiana pamoja na mfalme asirudi kwangu kwa nyumba ya Yonathan
nitakufa humo." 27 Kisha maafisa wote walikuja kwa Yeremia na kumuuliza, basi
aliwajibu kama mfalme alivyomuelekeza. Basi waliacha kuongea pamoja naye, kwa

sababu hawakusikia mazungumzo kati ya Yeremia na mfalme. 28 Basi Yeremia alibaki
kwenye uwanja wa mlinzi mpaka siku ile Yerusalem ilipotekwa.

# 39

1 Katika mwaka wa tisa na mwezi wa kumi wa Sedekia mfalme wa Yuda,
Nebukadreza mfalme wa Babeli alikuja pamoja na jeshi lake lote dhidi ya Yerusalem
na kuizingira. 2 Katika mwaka wa kumi na moja na mwezi wa nne wa Sekeia, siku ya
tisa ya mwezi, mji uliharibiwa. 3 Kisha maafisa wote wa mfalme wa Babeli walikuja
na kukaa kwenye lango la katikati: Nergali Sharezeri, Samgari Nebo, na Sarsechimu,
afisa muhimu. Nerga Sharezeri alikuwa afisa mkuu na wote waliobaki maafisa wa
mfalme wa Babeli. 4 Ilitokea kwamba wakati Sedekia, mfalme wa Yuda, na wanaume
wapiganaji wake wote walipowaona, walikimbia. Walitoka nje usiku toka kwenye mji
kwa njia ya bustani ya mfalme, kupitia lango la kati la kuta mbili. Mfalme alitoka nje
katika mwelekeo wa Arabah. 5 Lakini jeshi la Wakaldayo walimfatilia na kumpata
Sedekia kwenye tambarare za mto Yordani karibu na Yeriko. Kisha walimshika
na kumleta kwa Nebukadreza, mfalme wa Babeli, Riblah kwenye nchi ya Hamath,
ambapo Nebukadreza alipitisha sentensi juu yake. 6 Mfalme wa Babeli alimchinja
binti wa Sedekia mbele ya macho yake huko Ribla. Pia aliwachinja wanaume wote
wa heshima wa Yuda. 7 Kisha alingoa macho ya Sedekia na kumfunga mnyororo wa
shaba ili kusudi kumpeleka Babeli. 8 Kisha Wakaldayo walichoma nyumba ya mfalme
na nyumba za watu. Pia walivunja kuta za Yerusalem. 9 Nebukadreza, nahodha wa
walinzi wa mfalme, waliwachukua katika mateka watu wengine waliobaki katika
mji. Hii ilijumuisha watu waliotoka jangwa kwenda Wakaldayo na watu wengine
walioachwa katika mji. 10 Lakini Nebukadreza nahodha wa walinzi wa mfalme
aliwaruhusu watu maskini ambayo hawakuwa na chochote wao kubaki katika chi ya
Yuda. Aliwapa mashamba ya mizabibu na maeneo katika siku ile. 11 Nebukadreza
mfalme wa Babeli alikuwa ametoa amri kuhusu Yeremia kwa Nebuzaradani nahodha
wa walinzi wa mfalme. Alikuwa amesema, 12 “Mchukue na umjali. Usimdhuru.
Fanya kwa ajili yake chochote anachokuambia.” 13 Basi Nebuzaradani nahodha wa
walinzi wa mfalme, Nebushazbani mkuu wa matoashi, Nergali Sharezeri afisa mkuu,
na wote maafisa wa muhimu wa mfalme wa Babeli walituma watu nje. 14 Watu
wao walimchukua Yeremia kutoka uwanja wa mlinzi na kumkabidhi kwa Gedalia
mwana wa Ahikami mwana wa Shafani, kumchua nyumbani, basi Yeremia alibaki
miongoni mwa watu. 15 Sasa neno la Yahwe lilikuwa limekuja kwa Yeremia wakati
alipokuwa chini ya kifungo kwenye uwanja wa mlinzi, na alisema, 16 “Zungumza
kwa Ebedi Meleki Mkushi na sema, 'Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israel, asema
hivi: Ona, Nimekaribia kubeba maneno yangu dhidi ya mji huu kwa ajili ya janga
na si kwa uzuri. Kwa kuwa yatakuwa kweli mbele yako katika siku hiyo. 17 Lakini
nitakuokoa katika siku hiyo - hili ni tamko la Yahwe - na hautatiwa katika mkono
wa wanaume ambayo unawaogopa. 18 Kwa kuwa nitakuokoa hakika. Hautaanguka
kwa upanga. Utatoroka pamoja na maisha yako, kwani unanitumaini - hili lilikuwa
tamko la Yahwe.”

# 40

1 Hili lilikuwa neno ambalo lilikuja kwa Yeremia toka kwa Yahwe baada ya
Nebuzaradni, amri wa walinzi wa mfalme, amemtuma mbali kutoka Ramah. Huko
ndiko Yeremia alikuwa amechukuliwa, na huko alikuwa amefungwa kwa minyororo.
Alikuwa miongoni mwa mateka wote ya Yerusalem na Yuda ambayo walipaswa
kuwa matekani Babeli. 2 Mlinzi mkuu alimchukua Yeremia na kusema kwake,
“Yahwe Mungu wako aliamrisha maafa haya dhidi ya eneo hili. 3 Basi Yahwe alileta.
Alifanya kama alivyoamrisha, kwani ninyi watu mmefanya dhambi dhidi yake na

hamkutii sauti yake. Hii ni sababu ya jambo hili limetokea kwenu. Lakini sasa
tazama! 4 Nimekuacha huru leo toka kwenye minyororo iliyokuwa kwenye mikono
yako. Kama ni vizuri katika macho yako kuja nami Babeli, njoo, na nitakujali.
Lakini kama si vizuri katika macho yako kuja pamoja nami, basi usifanye hivyo.
Tazama nchi yote mbele yako. Nenda ambapo ni pazuri na sawa katika macho yako
kwenda." 5 Wakati Yeremia hakujibu, Nebuzaradani alisema, "Nenda kwa Gedalia
mwana wa Ahikam mwana wa Shafani, ambaye mfalme wa Babeli amemweka
msimamizi wa miji ya Yuda. Baki pamoja naye miongoni mwa watu au nenda
popote ni pazuri katika macho yako kwenda." Amri wa walinzi wa mfalme alimpa
chakula na zawadi, na kisha akamtuma mbali. 6 Basi Yeremia alienda kwa Gedalia
mwana wa Ahikam, huko Mizpah. Alibaki pamoja naye miongoni mwa watu ambao
walibaki nyuma katika nchi. 7 Sasa baadhi ya amri wa wanawajeshi wa Yuda
ambao walikuwa bado katika uwanja- wao na watu wao - walisikia kuwa mfalme
wa Babeli alimfanya Gedalia mwana wa Ahikam, liwali juu ya nchi. Pia walisikia
kuwa amemweka kusimamia wanaume, wanawake, na watoto ambao walikuwa
watu maskini katika nchi, wale ambao hawakuwa wamechukuliwa mateka Babeli.
8 Basi walienda kwa Gedalia huko Mizpa. Hawa watu walikuwa Ishmaeli mwana
Nethania; Yonathan na Yonathani, wana wa Kareaa; Seraya mwana wa Tanhumethi;
wana wa Efai Netophathite; na Yezania mwana wa Mmaaka-wao na watu wao.
9 Gedalia mwana wa Ahikam mwana wa Shafan, alichukua kiapo kwao na kwa
watu wao, na kusema kwao, "Usiogope kuwatumikia maafisa wa Wakaldayo. Ishi
katika nchi na kumtumkia mfalme wa Babeli, na itakuwa vizuri kwenu. 10 Na
tazama, Ninaishi Mizpa kukutana pamoja na Wakaldayo waliokuja kwetu. Basi vuna
mvinyo, matunda ya kiangazi, na mafuta na viweke kwenye vyombo vyako. Uishi
katika miji ambayo umechukua." 11 Kisha Wayahudi wote katika Moabu, miongoni
mwa watu wa Ammoni, na katika Edomu, na katika kila nchi ilisikiwa kwamba
mfalme wa Babalei ameruhusu mabaki ya Yuda kubaki, kwamba alimteua Gedalia
mwana wa Ahikam mwana wa Shafani juu yao. 12 Basi Wayahudi wote walirudi
toka kila eneo ambako walikuwa wametawanyika. Walirudi kwenye nchi ya Yuda,
kwa Gedalia huko Mizpa. Walivuna mvinyo na matunda ya kiangazi kwa wingi.
13 Yonathan mwana wa Karea na amri wote wa jeshi katika uwanja walikuja kwa
Gedalia huko Mizpa. 14 Walisema kwake, "Haujui kuwa Baalis mfalme wa watu
wa Ammoni amemtuma Ishmael mwana wa Nethania kukuua?" Lakini Gedalia
mwana wa Ahikim hakuwaamini. 15 Basi Yonathan mwana wa Karea alizungumza
kwa siri kwa Gedalia huko Mizpa na kusema, "Niruhusu niende kumuua Ishmael
mwana wa Nethania. Hakuna atakaye nituhumu. Kwanini asikuue wewe? Kwanini
kuruhusu Yuda yote ambayo imekusanywa kwako kutawanyishwa na mabaki ya
Yuda kuharibiwa?" 16 Lakini Gedalia mwana wa Ahikam alisema kwa Yonathan
mwana wa Karea, "Usifanye jambo hili, kwa kuwa unasema uongo kuhusu Ishmael."

# 41

1 Lakini ilitokea kwamba katika mwezi wa saba Ishmael mwana wa Nethania
mwana wa Elishama, toka familia ya kifalme, na maafisa baadhi wa mfalme, walikuja
- wanaume kumi walikuwa pamoja naye - kwa Gedalia mwana wa Ahikam, huko
Mizpa. Walikula chakula pamoja hukp Mizpa. 2 Lakini Ishmael mwana wa Nethania,
na wanaume kumi ambao walikuwa pamoja naye waliinuka na kumvamia Gedalia
mwana wa Ahikam mwana wa Shafan, kwa upanga. Ishmael alimuua Gedalia,
ambaye mfalme wa Babeli alimweka kuwa msimamizi wa nchi. 3 Kisha Ishmael
aliwauwa Wayahudi wote ambao walikuwa pamoja na Gedalia huko Mizpa na
Wakaldayo wanaume wa kupigana kukutwa huko. 4 Kisha ilikuwa siku ya pili
baada ya kumuua Gedila, lakini hakuna moja aliyejua. 5 Wanaume baadhi walikuja

toka Shechem, toka Shiloh, na toka Samaria-wanaume semanini ambayo walikuwa
wamenyoa ndevu zao, walirarua nguo zao, na kujikata wenyewe- pamoja na chakula
cha sadaka na ubani katika mikono yao kwenda kwa nyumba ya Yahwe. 6 Basi
Ishmael mwana wa Nethania alienda toka Mizpa kukutana nao kama walivyoenda,
wakitembea na kulia. Kisha ilitokea kwamba kama alivyokutana nao, alisema nao,
"Njoo kwa Gedalia mwana wa Ahikam!" 7 Ilikuja kuwa kwamba wakati walipokuja
katika mji, Ishmaeil mwana wa Nethania aliwauwa na kuwatupa kwenye shimo,
yeye na wanaume ambao walikuwa pamoja naye. 8 Lakini palikuwa na wanaume
kumi miongoni mwao ambao walisema kwa Ishmael, " Usituue, kwa kuwa kuna
riziki zetu kwenye shamba: ngano na shayiri, mafuta na asili" Kwa hiyo hakuwauwa
pamoja na rafiki zao wengine. 9 Kisima ambacho Ishmael alitupa miili yote ya
waliokufa ambaye yeye na Gedalia waliwapiga, kilikuwa ni kilekile ambacho mfalme
Asa alichimba wakati alipokuwa akivamiwa na mfalme Baasha wa Israel. Ishmael
mwana wa Nethania alilijaza wale ambao walikuwa wameuawa. 10 Badae Ishmael
aliwashika watu wengine wote ambao walikuwa huko Mizpa, mabinti wa mfalme na
watu wote ambao walikuwa wameachwa huko Mizpa ambayo Nebuzaradani mlinzi
mkuu alikuwa amewakabidhi kwa Gedalia mwana wa Ahikam. Basi Ishmael mwana
wa Nethania aliwashika na kuvuka kwa watu wa Ammon. 11 Lakini Yonathani
mwana wa Karea na amri wote wa jeshi pamoja naye walisikia madhara yote ambayo
Ishmael mwana wa Nethania alikuwa amefanya. 12 Basi waliwachukua wanaume
wao na kwenda kupigana dhidi ya Ishmanel mwana wa Nethania. Walipigana
naye huko kwenye kisima kuu cha Gibeoni. 13 Kisha ilitokea kwamba wakati watu
wote ambao walikuwa na Ishmael kuona Yonathani mwana wa Karea na amri
wote wa jeshi ambao walikuwa pamoja naye, walikuwa na furaha. 14 Basi watu
wote ambao Ishmael alikuwa amewashika huko Mizpa waligeuka na kwenda kwa
Yonathani mwana wa Karea. 15 Lakini Ishmael mwana wa Nethania alitoroka na
wanaume wanane toka kwa Yonathani. Alienda kwa watu wa Ammon. 16 Yonathani
mwana wa Karea na amri jeshi pamoja naye walichukua toka Mizpa watu wote
ambao walikuwa wameokolewa kutoka kwa Ishmael mwana wa Nethania. Hii
ilikuwa baada ya Ishmael kuwa amemuuwa Gedalia mwana wa Ahikam. Yonathan
na rafiki zake walichukua wanaume shujaa, wanaume wapiganaji, wanawake na
watoto, na mtoashi ambaye alikuwa ameokolewa huko Gibeoni. 17 Kisha walienda na
kubaki kwa muda huko Geruthi Chimham, ambayo iko karibu Bethelemu. Walikuwa
wakienda Misri 18 kwa sababu ya Wakaldayo. Walikuwa wakiwaogopa kwani Ishmael
mwana wa Nethania alikuwa amemua Gedalia mwana wa Ahikam, ambaye mfamle
wa Babeli amewekwa kwenye usimamizi wa nchi.

# 42

1 Kisha amri wote wa jeshi na Yonathan mwana wa Karea, Jezania mwana wa
Hoshaia, na watu wote kutoka mdogo kwa mkubwa walimkaribia Yeremia nabii.
2 Walisema naye, "Acha maombi yetu yaje mbele yako. Omba kwa ajili yetu kwa
Yahwe Mungu wako kwa ajili ya watu hawa ambao wanabaki kwani tuko wachache
katika idadi, kama unavyoona. 3 Muulize Yahwe Mungu wako atuambia sisi njia
yakuendea na nini tufanye." 4 Basi Yeremia nabii alisema nao, "Nimewasikia,
Tazama, Nitaomba kwa Yahwe Mungu wenu kama mlivyoomba. Vyovyote Yahwe
ananijibu, Nitawambia. Sitawaficha chochote ninyi." 5 Walisema na Yeremia, "Na
Yawhe awe shahidi mkweli na mwaminifu dhidi yenu, kama hatutafanya kila kitu
ambacho Yahwe Mungu wenu anatuambia kufanya. 6 Hata kama ni vizuri au vibaya,
tutatii sauti ya Yahwe Mungu wetu, ambaye tunawatuma ninyi, ili kwamba iwe vizuri
pamoja nasi wakati tunatii sauti ya Yahwe Mungu wetu." 7 Basi ilitokea kwamba
baada ya siku kumi, neno la Yahwe lilikuja kwa Yeremia. 8 Kwa hiyo Yeremia

alimwita Yonathan mwana wa Karea na amri wote jeshi pamoja naye, na watu wote
kutoka mdogo kwa mkubwa. 9 Na alisema nao, “Yahwe, Mungu wa Israel, ambaye
umenituma mimi ili niweze kuweka maombi yako mbele zake. Yahwe asema hivi,
10 Kama mtarudi na kuishi katika nchi hii, basi nitawajenga na sitawararua chini;
Nitapanda na sitawangoa, kwa kuwa nitageuza maafa ambayo nimeleta juu yako.
11 Msimugope mfalme wa Babeli, ambaye mnamuogopa. Msimuogope-hili ni tamko
la Yahwe kwani niko pamoja nanyi kuwahifadhi na kuwaokoa toka mkono wake.
12 Kwa kuwa nitawapa rehema. Nitakuwa na huruma juu yenu, na nitawarudisha
kwenye nchi yenu. 13 Lakini tudhani kusema kwamba, “Hatutakaa katika nchi hii”-
kama hamtasikiliza sauti yangu, sauti ya Yahwe Mungu wenu. 14 Tudhani kwamba
mnasema, “Hapana! Tutaenda kwenye nchi ya Misri, ambayo hatutaona vita yoyote,
ambayo hatutasikia sauti ya tarumbeta, na hatutaona njaa ya chakula. Tutaishi
huko.” 15 Sasa sikiliza neno hili la Yahwe, wewe mabaki ya Yuda. Yahwe wa
majeshi, Mungu wa Israel, asema hivi, 'Kama kweli mtatoka kwenda Misri, kwenda
na kuishi huko, 16 basi upanga ambao mnauogopa utawapita huko kwenye nchi
ya Misri. Njaa ambayo mnawasiwasi nayo itawafatilia huko Misri. Na mtakufa
huko. 17 Basi itatokea kwamba wanaume wote waliondoka kwenda Misri kuishi
huko watakufa kwa upanga, njaa, au pigo. Hapatakuwa na mwathirika wao, hakuna
atakayetoroka maafa ambayo nitaleta juu yao. 18 Kwa kuwa Yahwe wa majeshi,
Mungu wa Israel, asema hivi: Kama gadhabu yangu na hasira yangu imemwanga juu
ya wakazi wa Yerusalem, kwa njia hiyo hasira yangu itamwangwa juu yenu kama
mtaenda Misri. Mtakuwa sababu ya hasira na hofu, sababu la kuzungumza laana, na
kitu kisichokuwa na heshima. Na hamtaona eneo hili tena.” 19 Basi Yeremia alisema,
“Yahwe amezungumza kuhusu ninyi - mabaki ya Yuda. Msiende Misri! Unajua kwa
hakika kwamba nimekuwa shahidi dhidi yenu leo. 20 Kwa kuwa mmejidanganya
vibaya wenyewe wakati mliponituma mimi kwenda kwa Yahwe Mungu wenu na
kusema, 'Omba kwa Yahwe Mungu wetu kwa ajili yetu. Kila kitu ambacho Yahwe
Mungu wetu asema, tuambie, na tutaibeba.' 21 Kwa kuwa nimekwisha toa taarifa
kwako leo, lakini hajusikiliza sauti ya Yahwe Mungu wenu au kwa chochote kuhusu
ambacho alinituma mimi kwako. 22 Basi sasa, utajua kwa hakika kwamba utakufa
kwa upanga, njaa, na pigo katika eneo ambalo ulitamani kwenda kuishi.”

# 43

1 Ilitokea kwamba Yeremia alimaliza kuhubiri kwa watu wote maneno yote ya
Yahwe Mungu wao kwamba Yahwe Mungu wao alimwambia kusema. 2 Azaria
mwana wa Hoshaia, Yonathani mwana wa Karea, na watu wenye kiburi walisema
kwa Yeremia, “Unasema uongo. Yahwe Mungu wetu hajakutuma wewe kusema,
'Usiende Misri kuishi huko.' 3 Kwa kuwa Baruku mwana wa Neria anakuchochea
dhidi yetu kututoa sisi kwenye mkono wa Wakaldayo, kwa kuwa wewe umesababisha
kifo chetu na kutufanya sisi mateka huko Babeli.” 4 Basi Yonathani mwana
wa Karea, wakuu wa jeshi, na watu wote walikataa kusikiliza sauti ya Yahwe
kuishi kwenye nchi ya Yuda. 5 Yonathani mwana wa Karea na amri jeshi wote
waliwachukua mabaki wa Yuda ambao walikuwa wamerudi kutoka mataifa yote
ambapo walikuwa wametawanyika kuishi katika nchi ya Yuda. 6 Waliwachukua
wanaume na wanawake, watoto na mabinti wa mfalme, na kila mtu ambaye
Nebuzaradani, nahodha wa walinzi wa mfalme, waliruhusu kubaki pamoja na
Gedali mwana wa Ahikam mwana wa Shafan. Pia walimchukua Yeremia nabii na
Baruku mwana wa Neria. 7 Walienda nchi ya Misri, kwa Tahpanhesi, kwa sababu
hawakusikiliza sauti ya Yahwe. 8 Basi neno la Yahwe lilikuja kwa Yeremia huko
Tahpanhesi na kusema, 9 “Chukua mawe makubwa mkononi mwako, na, kwenye
macho ya watu wa Yuda, yafiche kwenye chokaa kwenye njia ya kuingia katika

nyumba ya Farao huko Tahpanhesi. [10] Kisha wakasema nao, “Yahwe wa majeshi,
Mungu wa Israel, asema hivi, 'Ona, nimekaribia kutuma wajumbe kumchukua
Nebukadreza mfalme wa Babeli kama mtumwa wangu. Nitaweka kiti cha enzi
juu ya mawe haya ambayo wewe, Yeremia, umeyazika. Nebukadreza ataweka
banda lake juu yao. [11] Kwa kuwa atakuja na kuvamia nchi ya Misri. Yeyote
aliyeandikiwa kufa atakufa. Yeyote aliyeandikiwa mateka atachukuliwa mateka. Na
yeyote aliyeandikiwa kwa upanga atakufa kwa upanga. [12] Kisha nitawasha moto
katika mahekalu ya miungu ya Misri. Nebukadreza atawachoma na kuwashika.
Atasafisha nchi ya Misri kama wachungaji wanavyosafisha wanyama waharibio nguo
zao. Ataenda nje kutoka eneo hilo kwa ushindi. [13] Atavunja nguzo za mawe huko
Heliopolisi kwenye nchi ya Misri. Atachoma mahekalu ya miungu ya Misri.”

# 44

[1] Hili lilikuwa neno ambalo lilikuja kwa Yeremia kuhusu Wayahudi wote walioishi
katika nchi ya Misri, wale wanaoishi Migdoli, Tahpanhesi, Memphis, na katika
nchi ya Patrosi. [2] “Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israel, asema hivi: Wewe
mwenyewe umeyaona maafa yote niliyoleta juu ya Yerusalemu na miji yote ya
Yuda. Ona, ni ukiwa leo. Hakuna yeyote anaishi mwao. [3] Hii ni kwa sababu
ya mambo maovu waliyofanya kunikosea mimi kwa kwenda kuchoma ubani na
kuabudu miungu mengine. Hawa walikuwa miungu ambao wala wao wenyewe,
wala ninyi, wala mababu zenu walijua. [4] Basi nirudie kuwatuma watumwa wangu
wote manabii kwao. Niliwatuma wao kusema, 'Acha kufanya vitu hivi machukizo
ambayo nachukia. [5] Lakini hawakunisikiliza. Walikataa kuwa makini au kuyaacha
maovu kwa kuchoma ubani kwa miungu mingine. [6] Basi hasira yangu na gadhabu
yangu zilimwanga na kuwasha moto kwenye miji ya Yuda na mitaa ya Yerusalemu.
Basi waliharibiwa na kuteketezwa, kama katika siku ya leo.” [7] Basi sasa Yahwe,
Mungu wa majeshi na Mungu wa Israel, asema hivi, “Kwanini unafanya maovu
makubwa dhidi yenu? Kwanini mnasababisha ninyi wenyewe kujitenga kutoka
miongoni mwa Yuda - wanaume na wanawake, watoto na wanyonyao? Hakuna
mabaki yenu yatabaki. [8] Kwa maovu yenu mmenikosea pamoja na matendo ya
mikono yenu, kwa kuchoma ubani kwa miungu mingine kwenye nchi ya Misri,
ambapo mmekwenda kuishi. Mmeenda huko ili kwamba mtaangamizwa, ili kwamba
mtalaaniwa na mashutumu miongoni mwa mataifa yote ya duniani. [9] Mmesahau
maovu yaliyofanywa na mababu zenu na maouvu yaliyofanywa na wafalme wa Yuda
na wake zao? Mmesahau uovu uliofanywa na ninyi na wake zenu katika nchi ya
Yuda na mitaa ya Yerusalemu? [10] Kwa siku hii, hawajanyenyekea bado. Hawashimu
sheria yangu au maagizo niliyoweka mbele yao na mababu zao, wala hawatembei
nazo.” [11] Kwa hiyo sasa Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israel, asema hivi, “Ona,
Nimekaribia kuweka uso wangu dhidi yenu kuleta maafa kwenu na kuiharibu Yuda
yote. [12] Kwa kuwa nitachukua mabaki wa Yuda ambaye ameanza safari kwenda
nchi ya Misri kuishi huko. Nitafanya hivi ili kwamba wataangamia wote katika
nchi ya Misri. Wataanguka kwa upanga na njaa. Kutoka wadogo kwa wakubwa
wataangamia kwa upanga na njaa. Watakufa na watakuwa sababu ya kuaapa,
kulaani, mashutumu, na kitu kibaya. [13] Kwa kuwa nitawaadhibu watu wakazi wa
nchi ya Misri kama nilivyoadhibu Yerusalem kwa upanga, njaa, na pigo. [14] Hakuna
mkimbizi au mwathirika wa mabaki ya Yuda ambaye wataenda kuishi huko kwenye
nchi ya Misri watarudi kwenye nchi ya Yuda, hata kama wanataka kurudi na kuishi
huko. Hakuna kati yao atarudi, ijapokuwa wachache ambayo watatoroka kutoka
huko.” [15] Kisha watu wote ambao walijua kwamba wake zao walikuwa wakichoma
ubani kwa miungu mingine, na wanawake wote waliokuwa katika kusanyiko kuu, na

watu wote ambao walikuwa wakiishi kwenye nchi ya Misri katika Pathrosi walimjibu
Yeremia. [16] Walisema, “Kuhusu neno ambalo mmetuambia sisi kwa jina la Yahwe:
Hatutakusikiliza. [17] Kwa hakika tutafanya mambo yote ambayo tulisema tungefanya:
kuchoma ubani kwa malkia wa Mbingu na kumwaga kinywaji cha sadaka kwake
kama sisi, mababu zetu, wafalme wetu, na viongozi wetu walivyofanya kwenye
miji ya Yuda na mitaa ya Yerusalemu. Kisha tutajazwa pamoja na chakula na
tutafanikiwa, pasipo kupata maafa yoyote. [18] Wakati tunajiepusha kutofanya mambo
haya, si kutoa sadaka ya ubani kwa Malkia wa Mbinguni na si kumwanga kinywaji
cha sadaka kwake, tulikuwa wote tunaumwa umaskini na tulikuwa tunakufa kwa
upanga na njaa.” [19] Wanawake walisema, “Wakati tulipokuwa tunatengeneza ubani
wa sadaka mbele ya Malkia wa Mbinguni na kumwaga kinywaji cha sadaka kwake,
tulifanya hivi vitu pasipo waume wetu kujua.” [20] Kisha Yeremia alisema kwa watu
wote - kwa wanaume na wanawake, na watu wote waliomjibu yeye - alihubiri na
kusema, [21] “Je Yahwe hakukumbuka ubani ambao mliuchoma kwenye miji ya Yuda
na mitaa ya Yerusalem - wewe na mababu zenu, wafalme wenu na viongozi, na watu
wa nchi? Kwa kuwa Yahwe anakumbuka hili kwenye akili; inakuja kwenye mawazo
yake. [22] Basi hawakuweza tena kuvumilia kwa sababu ya matendo yenu maovu, kwa
sababu machukizo ambayo mlifanya. Basi nchi yenu imekuwa ukiwa, kutisha, na
laana basi hapakuwa na mkazi tena kwa siku hii. [23] Kwa sababu mlichoma ubani
na kufanya dhambi dhidi ya Yahwe, na kwa sababu msingesikiliza sauti yake, sheria
yake, amri zake, au maagizo ya agano lake, maafa haya dhidi yenu yemetokea kama
kwa siku hii. “ [24] Kisha Yeremia alisema kwa watu wote na wanawake wote, “ Sikia
neno la Yahwe, Yuda yote ambao wamo katika nchi ya Misri. [25] Yahwe wa majeshi,
Mungu wa Israel, asema hivi, Wewe na wake zako wote mmesema kwa vinywa vyenu
na kubeba kwa mikono yenu kile mlichosema, “ Hakika tutabeba viapo ambavyo
tulifanya kumwabudu Malkia wa Mbinguni, kwanga kinywaji cha sadaka kwake.”
Sasa timiza viapo vyenu, vibebe.” [26] Basi, sikiliza neno la Yahwe, Yuda yote ambao
mnaishi katika nchi ya Misri, 'Ona, Nimeapa kwa jina langu kuu-asema Yahwe. Jina
langu halitaitwa kwa vinywa vya wanaume wowote wa Yuda kwenye nchi ya Misri,
wewe ambaye sasa unasema, “Kama Bwana Yahwe aishivyo.” [27] Ona, Ninakutazama
juu yako kwa ajili ya maafa na si kwa uzuri. Kila mtu wa Yuda katika nchi ya Misri
ataangamia kwa upanga na njaa mpaka wote wameishia. [28] Kisha waathirika wa
upanga watarudi kutoka nchi ya Misri kwa nchi ya Yuda, peke idadi ndogo yao. Basi
mabaki yote ya Yuda walioenda kwenye nchi ya Misri kuishi huko watajua ambao
neno litakuwa kweli: yangu au yao. [29] Hii itakuwa ishara kwa ajili yako - hili ni
tamko la Yahwe - kwamba ninaweka dhidi yenu katika eneo hili, ili kwamba mtajua
kwamba maneno yangu hakika yatawavamia pamoja na maafa. [30] Yahwe asema hivi,
'Tazama, ninakaribia kumtoa Farao Hofra mfalme wa Misri kwenye mkono wa adui
zake na kwenye mkono wa wale wanaotafuta kumuua. Itakuwa sawa kama wakati
nilimpa Sedekia mfalme wa Yuda kwenye mkono wa Nebukadreza mfalme wa Babeli,
adui wake aliyetafuta maisha yake.

# 45

[1] Hili ni neno ambalo Yeremia nabii alimwambia Baruku mwana wa Neria. Hii
ilitokea wakati alipoandika kwenye kitabu maneno haya kwa imla ya Yeremia - hii
ilikuwa katika mwaka wa nne wa Yehoyakimu mwana wa Yosia, mfalme wa Yuda,
na alisema, [2] “Yahwe, Mungu wa Israel, asema hivi kwako, Baruku: [3] Umesema,
Ole mimi, kwa kuwa Yahwe ameongeza uchungu wa maumivu. Kuugua kwangu
kumenichosha; sipati pumziko.' [4] Hivi ndivyo unapaswa kusema kwake: “Yahwe
asema hivi: Ona, nilichojenga, sasa ninararua chini. Nilichopanda, sasa ninangoa.

Hii ni kweli juu ya dunia. [5] Lakini unategema mambo makubwa kwa ajili yako?
Usitegemee hayo. Uone, maafa yanakuja kwa binadamu wote - hii ni tamko la Yahwe
- lakini ninakupa maisha yangu kama nyara popote utakakoenda."

## 46

[1] Hili ni neno la Yahwe lililomjia Yeremia nabii juu ya mataifa. [2] Juu ya Misri;
"Hili ni juu ya jeshi la Farao Neko, mfalme wa Misri aliyekuwako Karkemishi
kando ya mto Frati. Hili ni jeshi alilolishinda Nebukadneza mfalme wa Babeli
likishindwa katika mwaka wa nne wa Yehoyakimu mwana wa Yosia, mfalme wa
Yuda: [3] Wekeni tayari ngao ndogo na kubwa, na msonge vitani. [4] Watieni farasi lijamu
na hatamu, na mpande juu yao, ninyi wapanda farasi. Jiwekeni mahali penu, mkiwa
mmevaa helmeti vichwani mwenu. Inoweni mishale yenu na kuvaa silaha zenu.
[5] Ninaona nini hapa? Wana woga na wanakimbia, maana askari wao wameshindwa.
Wanakimbia kwa usalama na hawaangalii nyuma. Kitisho kipo mahali pote - hili ni
tamko la Yahwe - [6] wepesi hawawezi kukimbia, na askari hawezi kukwepa. Wana
jikwaa kaskazini na kuanguaka kando ya mto Frati. [7] Ni nani hawa wainukao kama
Nile, ambao maji yao yanaruka juu na chini kama mito? [8] Misri huinuka kama
mto Nile, na maji yake yanaumuka juu na chini kama mito. Anasema, 'nitapanda
juu; nitaifunika nchi. Nitaiharibu miji na watu wake. [9] Inukeni, farasi. Mwe na
hasira, ninyi vibandawazi. Askari na waende, Kushi na Putu, watu walio na ujuzi
wa ngao, na Ludimu, watu wenye ujuzi wa kupiga pinde zao. [10] Siku hiyo itakuwa
siku ya kisasi kwa Bwana Yahwe wa majeshi, naye atajilipizia kisasa juu ya adui zake.
Upanga utararua na kujirishisha. Utakula na kujishibisha kwa damu yao. Kwa maana
kutakuwa na sadaka kwa Bwana Yahwe wa majeshi katika nchi ya kaskazini kando ya
mto Frati. [11] Panda Gileadi ujipatie dawa, binti wa Misri uliyebikra. Haifai kwamba
unaweka dawa nyingi juu yako. Hakuna uponyaji kwako. [12] Mataifa wamesikia
kuaibika kwako. Nchi imejawa na maombolezo yako, maana askari anajikwaa juu
ya askari; na wote wawili uanguka pamoja." [13] Hili ndilo neno Yahwe alilomwambia
nabii Yeremia wakati Nebukadneza mfalme wa Babeli alipokuja na kushambulia nchi
ya Misri: [14] Toa taarifa kwa Misri na isikiwe katika Migdoli na Memfisi. Wamesema
katika Tapenesi, wekeni kituo na mwe imara, kwa maana upanga unakula wote kati
yenu. [15] Kwa nini Apisi mungu wenu amekimbia? Kwa nini ng'ombe dume mungu
wenu hakuweza kusimama? Yahwe amemwangusha chini. [16] Ameongeza idadi ya
waliojikwaa. Kila askari anaanguka kinyume cha anayefuata. Wanasema, "Inuka.
Haya twende nyumbani. Haya na turudi kwa watu wetu, katika nchi yetu ya asili.
Na tuuache upanga huu unaotuuwa." [17] Walitangaza pale, "Farao mfalme wa Misri ni
kelele tu, ameuacha wasaa wake mbali." [18] Kama niishivyo - hili ni tamko la mfalme
- Yahwe wa majeshi kwa jina, kuna mtu atakuja aliye kama Mlima Tabori na Mlima
Karmeli kando ya bahari. [19] Wekeni masanduku yenu kuyachukua uhamishoni, binti
mwishio Misri. Kwani Memfisi haitafaa, magofu. Hakuna atakayeishi huko. [20] Misri
ni mtamba mzuri sana, lakini mdudu aumaye anakuja kutoka kaskazini. Anakuja.
[21] Askari wake wakukodiwa ni kama dume la ng'ombe lililonona kati yake. lakini wao
pia watageuka na kukimbia. Hawatasimama pamoja, kwani siku yao ya madhara
inakuja kunyume chao, wakatik wa kuadhibiwa kwao. [22] Misri anatoa sauti kama
ya nyoka na kuondoka kwa kutambaa. maana adui yake anajiandaa kinyume chake.
Wanamkabili kama mkata miti aliye na shoka. [23] Wataangusha misitu - japokuwa ni
mingi sana - hili ni tamko la Yahwe. Kwa maana adui watakuwa wengi kuliko nzige,
wasiohesabika. [24] Binti Misri ataaibishwa. Atawekwa mkononi mwa watu kutoka
kaskazini." [25] Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli, asema, "Tazama, niko karibu
kumwadhibu Amoni wa Thebesi, Farao, Misri na miungu yake, Farao mfalme wake,

na wote wanaomtumaini. 26 Nitawaweka katika mkono wa wanaoyaona maisha yao,
na katika mkono wa Nebukadneza mfalme wa Babeli na watumishi wake. Kisha
baada ya haya Misri itakaliwa kama mwanzo - asema Yahwe." 27 Lakini, wewe Yakobo
mtumishi wangu, usihofu. Usifadhaike, Israeli, maana tazama, nitakurudisha kutoka
mbali, na uzao wako kutoka nchi ya mateka. Kisha Yakobo atarudi, tafuta amani,
na kuwa salama, na hapatakuwa na wa kumwogofya. 28 Wewe, mtumishi wangu
Yakobo, usiogope - asema Yahwe - kwa maana nipo nawe, hivyo nitaleta maangamizi
makamilifu dhidi ya mataifa yote nilikokupeleka. Lakini sitakuharibu kabisa. Hata
hivyo nitakuadhibu kwa haki na hakika sitakuacha bila adhabu."

# 47

1 Hili ni neno la Yahwe lililokuja kwa Yeremia nabi juu ya Wafilisiti. Neno
hili lilimjia kabla Farao hajaishambulia Gaza. 2 "Yahwe asema hivi: Tazama,
mafuriko ya maji yanainuka huko kaskazini. Yatakuwa kama mto uliofurika! Kisha
yataigharikisha nchi na kila kitu ndani yake, miji yake na watu wakaao ndani yake!
Kila mtu atapiga kelele ya kuomba msaada, na wakaaji wote wa nchi wataomboleza.
3 Kwa sauti ya kukanyaga kwa kwato za farasi wao wenye nguvu, kwa mwungurumo
wa vibandawazi vyao na kelele za magurudumu yao, wazazi hawatawasaidia watoto
wao kwa sababu ya udhaifu wao. 4 Kwa maana siku inakuja itakayowaacha ukiwa
Wafilisiti wote, kumwondoa kila mtu aliyesalia anayetaka kuwasaidia. Kwa maana
Yahwe anawaangamiza Wafilisiti, waliosalia katika kisiwa cha Kaftori. 5 Maombolezo
yatakuja juu ya Gaza. Hata kwa Ashikeloni, watu waliosalia bondeni watakuwa
kimya. Ni kwa muda gani mtajiondoa katika maombolezo? 6 Ole, upanga wa
Yahwe! itachukua muda gani hata unyamaze? Rudini alani mwenu! Acha na
unyamaze. 7 Wawezaje kuwa kimya, maana Yahwe amekuagiza. Amekuamuru
kumpiga Ashikeloni na dhidi ya nchi ya pwani ya bahari.

# 48

1 Juu ya Moabu, Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli, asema hivi, "Ole kwa
Nebo, kwani umekuwa ukiwa. Kiriathaimu umetekwa na kuaibishwa. Ngome zake
zimeangushwa na kuaibishwa. 2 Heshima ya Moabu haipo tena. Adui zake katika
Heshboni walipanga njama za kumwangamiza. Walisema, 'Njoni tumwangamize
kama taifa. Madmena pia itaangamizwa - upanga utakutangulia.' 3 Sikilizeni!
Sauti ya mvumo inakuja kutoka Horonaimu. 4 Moabu ameangamizwa. Vilio vya
watoto wake vinasikika. 5 Wanapanda kilima cha Luhithi wakilia, njia yote kuelekea
Horonaimu, vilio vinasikika kutokana na maangamizi. 6 Kimbieni! okeeni maisha
yenu kama kichaka cha mreteni katika nyika. 7 Maana kwa sababu ya tumaini lenu
katika matendo na utajiri wenu, ninyi pia mtatekwa. Kisha Kemoshi atachukuliwa
matekani, pamoja na makuhani na viongozi wake. 8 Maana mwaribu atafika kila
mji; hakuna mji utakaookoka. Hivyo bonde litaangamia na tambarare itateketezwa,
kama alivyosema Yahwe. 9 Mpeni Moabu mabawa, maana ni lazima aruke mbali bila
shaka. Miji yake itakuwa magofu, pasipo na mtu wa kuishi humo. 10 Na alaaniwe
kila aliye mvivu katika kufanya kazi ya Yahwe! Na alaaniwe kila auzuiaye upanga
wake usimwage damu! 11 Moabu amekuwa akijisikia salama tangu alipokuwa kijana.
Yeye ni kama mvinyo wake ambao haujamiminwa kutoka mtungi kwenda mtungi
mwingine. Hajaenda matekani. Hivyo radha yake ni njema kama mwanzo; radha
yake haibadiliki. 12 Hivyo tazama, siku zinakuja - asema Yahwe - nitakapompelekea
watakao mchovya na kumwaga mitungi yake yote na kupasua mitungi yake. 13 Kisha
Moabu atamwaibikia Kemoshi kama ambavyo nyumba ya Israeli ilivyoiabikia Betheli,
tumaini lao. 14 Utawezaje kusema, 'Tu askari, wapiganaji wenye nguvu'? 15 Moabu

itaangamizwa na miji yake kushambuliwa. Kwa maana vijana wake wazuri
wameshuka katika eneo la machinjo. Hili ni tamko la mfalme! Yahwe wa majeshi
ndilo jina lake. 16 Maangazizo ya Moabu yanakaribia; maafa yanaharakisha. 17 Ninyi
nyote mlio karibu na Moabu, ombolezeni. Nanyi mjuao fahari yake, pigeni kelele
hivi, 'Ole, fimbo yenye nguvu, fimbo yenye heshima, imevunjwa.' 18 Shukeni kutoka
mahali penu pa heshima na kuketi katika nchi kavu, ewe binti uishie Diboni. Maana
aiangamizaye Moabu anakushambulia, atakayeziharibu ngome zako. 19 Simameni
njiani na kuangalia, enyi mwishio katika Aroeri. Waulizeni wanaokimbia na
kutoroka. Sema, 'Nini kimetokea?' 20 Moabu ameaibika, maana amevujwa. Lieni kwa
sauti na uchungu; pigeni yowe kuomba msaada. Wambieni watu waliokando ya Mto
Arinoni kwamba Moabu ameangamizwa. 21 Basi maangamizi yamefika katika nchi ya
kilima, huko Holoni, Yakza, na Mefathi, 22 huko Diboni, Nebo, na Bethi Diblathaimu,
23 huko Kiriatahaimu, Beth Gamul, na Bethi Meoni, 24 huko Keriothi na Bozra, na
katika miji yote iliyomo katika nchi ya Moabu - miji iliyoko mbali na karibu. 25 Nguvu
za Moabu zimekwisha; mkono wake umevunjwa - asema Yahwe. 26 Mnywesheni,
maana alitenda kwa kiburi kinyume changu, Yahwe. Basi Moabu anapiga makofi kwa
machukizo kwa matapiko yake mwenyewe, hivyo amekuwa pia kitu cha kuchekesha.
27 Maana Israeli hakuwa kitu cha kuchekesha kwako? Alionekana miongoni mwa
wezi, kwamba ulitikisa kichwa chako kwake mara ulipoongea juu yake? 28 Jitengeni
na miji na kuweka kambi katika minuko, enyi watu wa Moabu. Kuwa kama njiwa
anayeatamia juu ya mlango wa tundu katika miamba. 29 Tumesikia juu ya kiburi cha
Moabu - majivuno yake, maringo, kiburi, utukufu binafsi na kujiinua moyoni. 30 Hili
ni tamko la Yahwe - mimi mwenyewe najua maneno yake ya ukaidi, yasiyosaidia
chochote, kama matendo yake. 31 Hivyo nitavumisha maombolezo kwa ajili ya
Moabu, na nitapiga kelele katika uzuni kwa ajili ya Moabu. Nitaomboleza kwa
ajili ya watu wa Kir Hereshi. 32 Nitalia zaidi kwa ajili yenu kuliko nilivyofanya
kwa Yazeri, mzabibu wa Sibma! Matawi yako yalipita katika Bahari ya Chumvi na
kufika hata Yazeri. Mwaribu ameshambulia matunda yenu ya kiangazi na mzabibu
wenu. 33 Hivyo sherehe na furaha vimeondolewa kutoka miti ya matunda na nchi ya
Moabu. Nimekomesha mvinyo kutoka mashinikizo yao. Hawatakanyaga kwa kelele
za furaha. Kelele yoyote haitakuwa kelele ya furaha. 34 Kutoka kelele huko Heshiboni
hata kufika Eleale, sauti yao inasikika hata Yahazi, kutoka Soari hata Horonaimu na
Eglathi Shelishiya, hata maji ya Nimrimu yamekauka. 35 Maana nitamkomesha kila
mtu katika Moabu atoaye sadaka mahali pa juu na kuteketeza uvumba kwa miungu
yake - asema Yahwe. 36 Hivyo moyo wangu unamwombolezea Moabu kama zomari.
Moyo wangu unaomboleza kama zomari kwa ajili ya watu wa Kir Heresi. Utajiri
walioupata umekwisha. 37 Maana kila kichwa kina upaa na kila kidevu kimenyolewa.
Chale zipo katika kila mkono, na nguo za magunia katika viuno vyao. 38 Maombolezo
yapo kila mahali, juu ya kila paa la nyumba ya Moabu na katika masoko ya Moabu.
Kwa maana nimeivunja Moabu kama chungu kisichotakiwa tena - asema Yahwe.
39 Jinsi gani imeharibiwa! Jinsi wanavyopiga kelele katika maombolezo yao! Moabu
ameigeuza kwa aibu! Hivyo Moabu atakuwa kitu cha kuchekwa na kitisho kwa wote
wanaomzunguka." 40 Maana Yahwe asema hivi, "Tazama, adui atakuja akiruka kama
tai, akieneza mabawa yake juu ya Moabu. 41 Keriothi umetekwa, na ngome zake
zimekamatwa. Maana siku hiyo myoyo ya askari wa Moabu itakuwa kama mioyo ya
wanawake katika uchungu wa kujifungua. 42 Hivyo Moabu utaharibiwa kama watu,
kwa kuwa walijivuna kinyume changu, Yahwe. 43 Hofu na shimo, na mtego vinakujia,
watu wa Moabu - asema Yahwe. 44 Kila akimbiaye kwa sababu ya hofu ataanguka
shimoni, na kila atokaye shimoni atanaswa na mtego, maana nitayaleta haya juu yao
katika mwaka wa kisasi changu dhidi yao - asema Yahwe. 45 Wakimbiao watasimama

katika kivuli cha Heshboni bila nguvu, maana moto utatoka Heshboni, miale kutoka
katikati ya Sihoni. Utateketeza paji la uso wa Moabu na juu ya vichwa vya watu
wenye majivuno. 46 Ole wako, Moabu! watu wa Kemoshi wameangamizwa, Kwa
maana wana wako wamechukuliwa kama mateka na binti zako matekani. 47 Lakini
nitazirejesha siku njema za Moabu katika siku zijazo - asema Yahwe.” Hukumu ya
Moabu inaishia hapa.

# 49

1 Juu ya watu wa Amoni, Yahwe asema hivi, “Je Israeli hana watoto? Je hakuna
mtu wa kurithi chochote katika Israeli? Kwa nini Moleki aikalie Gadi, na watu
wake kukaa katika miji yake? 2 Hivyo angalia, siku zinakuja - asema Yahwe -
nitakapo sikizisha ishara ya vita juu ya Raba miongoni mwa watu wa Amoni, hivyo
itakuwa rundo lililoachwa na binti zake watawasha moto. Maana Israeli atawamiliki
wanaommiliki,” asema Yahwe. 3 Piga kelele kwa maombolezo, Heshboni, maana Ai
utaangamizwa! Piga kelele, Binti za Raba! Vaeni nguo za magunia. Ombolezeni
na kukimbia kwa kuchanganyikiwa, maana Moleki anakwenda matekani, pamoja
na makuhani na viongozi wake. 4 Kwa nini mnajivunia nguvu zenu? Nguvu zenu
zitakwisha, binti wasioamini, ninyi mnaotumaini utajiri wenu. Mwasema, “Nani
atakayekuja kinyume changu?' 5 Tazama, nitaleta kitisho juu yenu - hili ni tamko
la Yahwe, Bwana wa majeshi - kitisho hiki kitatoka kwao wote wanaowazunguka.
Kila mmoja wenu atatawanyika mbele yake. Hakutakuwa na wa kuwakusanya
wanaotawanyika. 6 Lakini baada ya haya nitarejesha mema ya watu wa Amoni
- hili ni tamko la Yahwe.” 7 Juu ya Edomu, Yahwe wa majeshi asema hivi, Je
hakuna tena hekima katika Temani? Je ushauri mwema umepotea kutoka kwa
wenye ufahamu? Je hekima yao imeharibika? 8 Kimbieni! Rudini nyuma! Bakini
katika mashimo katika ardhi, wenyeji wa Dedani. Maana naleta maafa ya Esau
juu yake wakati ninaomwadhibu. 9 Ikiwa wavunaji wa zabibu walikuja kwako, je
wasinge acha kidogo? Ikiwa wezi walikuja usiku, je wasingeiba kiasi walichotaka?
10 Lakini nimempiga Esau kwa ukiwa. Nimefunua maficho yao. Hivyo hataweza
kujificha mwenyewe. Watoto wake, ndugu zake, na jirani zake wameharibiwa,
wamepotea. 11 Acha nyuma yatima wako. Nitachukua uhai wao, na wajane wako
wanaweza kuniamini.” 12 Maana Yahwe asema hivi, “Tazama, wasiostahili ni
lazima wanywe sehemu ya kikombe. Je mnadhani mtaachwa bila kuhadhibiwa?
Hapana, maana hakika mtakunywa. 13 Maana nimekwisha apa kwangu mimi
mwenyewe - asema Yahwe - Hiyo Bozra itakuwa hofu, aibu, magofu, na kitu cha
laana. Miji yake yote itakuwa magofu daima. 14 Nimesikia habari kutoka kwa
Yahwe, na mjumbe ametumwa katika mataifa, 'Kusanyikeni na kumpiga. Jiandaeni
kwa vita.' 15 “Maana tazama, nimekufanya kuwa mdogo kulinganisha na mataifa
mengine, yenye kudharauliwa na watu. 16 Na kwa hofu yenu, kiburi cha moyo
wako kimekudanganya, wakaaji wa maeneo ya mwinuko, ninyi mliomiliki vilele vya
vilima ili mfanye viota vyenu kama tai. Nitawashusha kutoka huko - asema Yahwe.
17 Edomu atakuwa kitisho kwa kila aipitaye. Kila mtu atatetemeka na kutoa sauti kwa
sababu ya maafa yake. 18 Kama maangamizi ya Sodoma na Gomora na jirani zake,”
asema Yahwe, “hakuna atakayeishi pale; hakuna mtu atakayekaa huko. 19 Tazama,
nitapanda kama simba kutoka katika misitu ya Yordani hata eneo la malisho mabichi.
Maana nitaharakisha kumfanya Edomu kumkimbia, nami nitamweka mwingine
atakayekuwa amechaguliwa kwa usimamizi huo. Maana ni nani aliyekama mimi,
ni nani atakayeniagiza kuja? Mchungaji gani awezaye kunizuia? 20 Hivyo sikiliza
mipango ambayo Yahwe ameamua dhidi ya Edom, mipango aliyoifanya kinyume cha
wakaao Temani. Bila shaka wataondolewa, hata kundi dogo kuliko yote. Nchi yao
yenye malisho yao mabichi itageuzwa kuwa sehemu zenye magofu. 21 Kwa kishindo

cha kuanguka kwao nchi hutikisika. Sauti ya milio ya kukata tamaa inasikika katika
Bahari ya Shamu. 22 Tazama, mtu fulani atapiga kama tai, na kushuka chini kwa
kasi na kueneza mabawa yake juu ya Bozra. Kisha katika siku hiyo, mioyo ya askari
wa Edomu itakuwa kama moyo wa mwanamke katika kuzaa." 23 Juu ya Dameski:
"Hamathi na Arpadi zitaaibika, maana wamesikia habari ya madhara. Wanayeyuka!
Wamesumbuka kama bahari, isiyotulia. 24 Dameski umekuwa dhaifu sana. Unageuka
kukimbia; hofu imeushika, Maangaiko na maumivu yameupata, kama uchungu wa
mwanamke ajifunguaye. 25 Watu wake wanasema, "Umekuwaje mji maarufu, mji
ambao nimeufurahia, kabla haujaachwa? 26 Kwa hiyo vijana wake wataanguka
katika mitaa yake na askari wake wote watateketea siku hiyo - hili ni tamko la Yahwe
wa majeshi." 27 "Maana nitawasha moto katika kuta za Dameski, nami nitazivunja
ngome za Beni Hadadi." 28 Juu ya Kedari na falme za Hazori, Yahwe amwambia hivi
Nebukadneza (Basi Nebukadneza mfalme wa Babeli alikuwa akienda kuyashambulia
maeneo haya): "Inuka na uipige Kedari na kuwaharibu wale watu wa mashariki.
29 Jeshi lake litachukua hema zao na makundi yao, nguzo za hema yao, na vitu vyao
vyote. Watachukua ngamia wao kutoka kwa watu wa Kedari na kuwambia, 'Hofu
ipo pande zote!" 30 Kimbia, Tangatanga mbali! Kaa katika maandaki ardhini, mkaao
Hazori - asema Yahwe - maana Nebukadneza mfalme wa Babeli amepanga mpango
kinyume chenu. Kimbieni! Geukeni! 31 Simama! lishambulie taifa lililokatika
amani, waishio salama," asema Yahwe. Hawana malango wala nguzo ndani yao,
na watu wake wanakaa wenyewe. 32 Maana farasi wao watakuwa mateka, na
wingi wa mali zao utakuwa mateka wa vita. Kisha nitawatawanya katika kila
upepo wanaonyoa pembe za nywele zao, nami nitaleta madhara juu yao kutoka
kila upande - hili ni tamko ya Yahwe. 33 Hazori utakuwa makao ya mbwea, nchi
isiyofaa daima. Hakuna atakayeishi huko; hakuna mwanadamu atakayekaa huko."
34 Hili ni neno la Yahwe lililomwijia Yeremia nabii kuhusu Elamu. Ilikuwa wakati
wa mwanzo wa kutawala kwake Sedekia mfalme wa Yuda, naye akasema, 35 "Yahwe
wa majeshi asema hivi: Tazama, ninakaribia kumvunja mpiga upinde wa Elamu,
sehemu kuu ya nguvu zao. 36 Maana nitaleta pepo nne kutoka katika pande nne
za mbingu, nami nitawatawanya watu wa Elamu katika pepo hizo zote. Hakuta
kuwa na taifa ambalo kwalo waliotawanywa kutoka Elamu hawatakwenda. 37 Hivyo
nitawavunjavunja Elamu mbele ya adui zao na mbele ya watafutao uhai wao. Maana
nitaleta maangamizo dhidi yao, hasira ya gadhabu yangu - hili ni tamko la Yahwe -
nami nitapeleka upanga nyuma yao hata nitakapowafuta wote. 38 Kisha nitaweka
kiti changu cha enzi huko Elamu na kumwangamiza mfalme na viongozi wao kutoka
huko - asema Yahwe - 39 na itakuwa siku zijazo kwamba nitarejesha mema ya Elamu
- asema Yahwe."

# 50

1 Hili ni neno alilolisema Yahwe juu ya Babeli, nchi ya Wakalidayo, kwa mkono
wa Yeremia nabii, 2 "Wajulishe mataifa ili wasikie. Toa ishara ili wasikie. Usiiache.
Sema, 'Babeli imetwaliwa. Beli ameaibika. Merodaki amefadhaika. Sanamu
zake zimeaibishwa; vinyago vyake vimefadhaika 3 Taifa kutoka kaskazini litainuka
kinyume chake, ili kuifanya nchi yake ukiwa. Hakuna hata mmoja, awe mtu au
mnyama, atakayeishi ndani yake. Wataondoka. 4 Katika siku hizo na wakati huo -
hili ni tamko ya Yahwe - watu wa Israeli na watu wa Yuda watakusanyika ili kwenda
kwa kulia na kumtafuta Yahwe Mungu wao. 5 Watauliza njia ya kwenda Sayuni
nao watakwenda huko, wakisema, tutakwenda wenyewe ili kuungana na Yahwe
katika agano la milele lisilosahaulikal 6 Watu wangu wamekuwa kondoo waliopotea.
Wachungaji wao wamewapoteza milimani; wamewageuza kutoka mlima hata

mlima. Walikwenda, wakasahau mahali walipokuwa wanaishi. [7] Kila awaendeaye
anawararua. Washitaki wao walisema, 'Hatuna hatia, kwa sababu walimtenda
dhambi Yahwe, nyumbani kwao halisi - Yahwe, tumaini la mababu zao.' [8] Tokeni
kati ya Babeli; tokeni katika nchi ya Wakalidayo; iweni kama wafanyavyo mabeberu
mbele ya kundi lote. [9] Maana tazama, ninaelekea kupeleka na kuinua kinyume cha
Babeli kundi la mataifa makubwa kutoka kaskazini. Yatajipanga yenyewe kinyume
chake. Kutoka hapo Babeli utatekwa. Mishale yao ni kama shujaa mzoefu asiyerudi
mikono tupu. [10] Ukaldayo itakuwa mateka. Wate waitekao wataridhika - asema
Yahwe. [11] Mnafurahi, mnasherehekea kuteka urithi wangu; mnarukaruka kama
ndama anayekanyaga katika malisho yake; mnalia kama farasi mwenye nguvu.
[12] Hivyo mama yenu ataaibika sana; aliyewazaa atafadhaika. Tazama, atakuwa wa
mwisho katika mataifa, nyika, nchi kame, na jangwa. [13] Kwa sababu ya hasira ya
Yahwe, Babeli haitakaliwa, lakini itakuwa ukiwa mtupu. Kila apitaye kando ataogopa
kwa sababu ya Babeli na atatoa sauti kwa sababu ya majeraha yake. [14] Jipangeni
wenyewe kumzunguka Babeli kinyume chake. Kila apindaye upinde na ampige.
Msizuie mshale wenu wowote, maana amemtenda dhambi Yahwe. [15] Pigeni kelele za
ushindi kinyume chake ninyi nyote mmzungukao. Amesalimu mamlaka yake; minara
yake imeanguka. Kuta zake zimebomolewa, maana hiki ni kisasi cha Yahwe. Jilipizeni
kisasi juu yake! Mtendeeni kama alivyoyatenda mataifa mengine. [16] Waaribuni wote
mkulima apandaye mbegu naye atumiaye mundu wakati wa mavuno katika Babeli.
Haya kila mtu na arudi kwa watu wake kutoka upanga wa mtesaji; na wakimbilie
katika nchi yao wenyewe. [17] Israeli ni kondoo aliyetawanywa na kupelekwa na
simba mbali. Kwanza mfalme wa Ashuru alimrarua; kisha baadaye, Nebukadneza
mfalme wa Babeli akavunja mifupa yake. [18] Kwa hiyo Yahwe wa majeshi, Mungu
wa Israeli, asema hivi: Tazama, nitamwadhibu mfalme wa Babeli na nchi yake,
kama nilivyomwadhibu mfalme wa Ashuru. [19] Nitamrudisha Israeli katika nchi yake;
atajilisha katika Karmeli na Bashani. Kisha atajishibisha katika nchi ya kilima ya
Efraimu na Gileadi. [20] Siku hizo na wakati huo, asema Yahwe, uovu utatafutwa katika
Israeli, lakini hautaonekana. Nitauliza kuhusu dhambi za Yuda, lakini hazitaonekana,
maana nitawasamehe mabaki niliowaacha." [21] Inuka dhidi ya nchi ya Merathaimu,
kinyume chake nao waishio Pekodi. Wapigeni kwa makali ya upanga na mwatenge
kwa ajili ya maangamizo - asema Yahwe - fanyeni kila ninachowaamru. [22] Sauti
ya vita na maangamizi ya kustaajabisha yamo katika nchi. [23] Jinsi gani nyundo
ya mataifa yote imekatiliwa mbali na kuharibiwa. Jinsi Babeli amekuwa kitu cha
kushangaza kati ya mataifa. [24] Nimetega mtego dhidi yako. Umenaswa, Babeli, nawe
haukutambua! Ulionekana na kukamatwa, tangu uliponidhihaki, Yahwe. [25] Yahwe
amefungua ghala lake la silaha na anachukua silaha kwa ajili ya kutekekeleza
hasira yake. Kuna kazi kwa ajili ya Yahwe wa majeshi katika nchi ya Wakaldayo.
[26] Mshambulie kutokea mbali. Fungua maghala yake ya chakula na kumrundika
kama marundo ya nafaka. Mtenge mbali na maangamizi. Usimbakizie masalia.
[27] Ua madume wake wote wa ng'ombe. Washushe sehemu ya machinjio. Ole wao,
maana siku yao imefika - wakati wa kuadhibiwa kwao. [28] Kuna sauti ya wale
wanaokimbia, walionusurika, katika nchi ya Babeli. Hawa watatoa taarifa ya kisasi
cha Yahwe Mungu wetu kwa Sayuni, kisasi kwa hekalu lake." [29] Ita wapiga pinde
dhidi ya Babeli - wale wote wapindao pinde zao. Piga kambi kinyume chake, na
msimwache yeyote kutoroka. Mlipeni kwa kile alichofanya. Mfanyieni kwa kipimo
alichotumia. Maana amemdharau Yahwe, Mtakatifu wa Israeli. [30] Hivyo vijana wake
wataanguka katika viwanja vya mji, na wapiganaji wake wote wataangamizwa siku
hiyo - hili ni tamko la Yahwe." [31] Tazama, mimi ni kunyume chako, mwenye majivuno
- hili ni tamko la Bwana Yahwe wa majeshi - maana siku yako imefika, mwenye

kiburi, wakati nitakapokuadhibu. 32 Hivyo wenye kiburi watajikwaa na kuanguka.
Hakuna atakaye wainua. Nitawasha moto katika miji yao; utateketeza kila kitu kati
yake. 33 Yahwe wa majeshi asema hivi: watu wa Israeli wamenyanyaswa, pamoja
na watu wa Yuda. Wate waliowateka bado wanawashikilia; wanakataa kuwaacha
waondoke. 34 Yeye awaokoaye ni mwenye nguvu. Yahwe wa majeshi ni jina lake.
Kwa hakika atalitetea shitaka lao, ili kuleta pumziko katika nchi, na kuwapiga wakaao
Babeli. 35 Upanga u juu ya Wakalidayo - asema Yahwe - na juu ya wakaao Babeli,
viongozi wake, na wenye hekima wake. 36 Upanga unakuja juu ya waganga, ili
wajione kuwa wajinga. Upanga utakuwa juu ya askari wake, hivyo watajaa hofu.
37 Upanga utakuwa juu ya farasi wake, vibandawazi vyao na na watu wote waliomo
Babeli, hivyo watakuwa kama wanawake. Upanga utakuwa juu ya ghala zake, nazo
zitatekwa. 38 Ukame unakuja juu ya maji yake, hivyo yatakauka. Maana ni nchi ya
miungu wasiofaa, na wanafanya kama watu waliofanywa punguani kwa miungu yao
isiyosaidia. 39 Hivyo wanyama wa jangwani wakaishi na mbwea wataishi huko, na
watoto wa mbuni wataishi ndani yake. Kwa muda wote, hatakaliwa tena. Kutoka
kizazi hata kizazi, hatakaliwa tena na watu. 40 Kama vile Mungu alivyoziangamiza
Sodoma na Gomora na majirani zake - asema Yahwe - hakuna atakayeishi huko;
hakuna mtu atakayekaa ndani yake." 41 "Tazama, watu wanakuja kutoka kaskazini,
maana taifa kubwa na wafalme wengi wamemtikisa kutokea mbali. 42 Watachukua
pinde na mishale. Ni wakatili na hawana huruma. Sauti yao ni kama mngurumo wa
bahari, na wamepanda farasi katika mpangilio kama watu wapiganao, dhidi yako,
bindi Babeli. 43 Mfalme wa Babeli amesikia habari yao na mikono yake imelegea
kwa huzuni. Mashaka yamemshika kama mwanamke katika utungu. 44 Tazama!
Anakwenda juu kama simba atokaye katika miinuko ya Yordani kuelekea katika eneo
la malisho ya uvumilivu. Maana kwa haraka nitawafanya wakimbie kutoka humo,
nami nitamweka mtu aliyechaguliwa kwa uangalizi wake. Maana ni nani aliye kama
mimi, na ni nani atakayeniagiza? Mchungaji gani awezaye kunizuia? 45 Sikilizeni
mipango ambayo Yahwe ameamua juu ya Babeli, mipango aliyonayo dhidi ya nchi
ya Wakaldayo. Kwa hakika wataondolewa, hata kundi dogo zaidi. Eneo lao la malisho
litageuzwa kuwa sehemu zenye magofu. 46 Kwa sauti ya kuangushwa kwa Babeli nchi
inatikisika, na sauti ya mateso yao inasikiwa kati ya mataifa."

# 51

1 Yahwe asema hivi: Tazama, ninakwenda kuleta upepo wa maangamizi dhidi
ya Babeli na dhidi yao waishio ndani ya Leb Kamei. 2 Nitawatuma Babeli wageni.
Watamtawanya na wataifanya ukiwa nchi yake, maana watakuja kinyume chake
kutoka pote siku ya madhara. 3 Msiwaache wapiga mishale wakapinda pinde zao;
msiwache wakavaa silaha zao. Msiwahifadhi vijana wake wa kiume; litengeni jeshi
lake lote kwa maangamizi. 4 Maana watu waliojeruhiwa wataanguka katika nchi
ya Wakaldayo; waliouawa wataanguka katika mitaa yake. 5 Maana Israeli na Yuda
hawajaachwa na Mungu wao, na Yahwe wa majeshi, japokuwa nchi yao imejaa
na maasi yaliyotendwa kinyume cha Mmoja aliye Mtakatifu wa Israeli. 6 Kimbieni
kutoka Babeli; kila mtu na ajiokoe mwenyewe. Msiangamie katika maasi yake.
Maana ni wakati wa kisasi cha Yahwe. Atamlipa kwa yote. 7 Babeli alikuwa
kikombe cha dhahabu mkononi mwa Yahwe kilichoinywesha nchi yote; mataifa
walikunywa mvinyo wake wakawa wendawazimu. 8 Babeli utaanguka ghafla na
kuangamizwa. Mwombolezeeni! mpeni dawa kwa maumivu yake; pengine aweza
kupona. 9 Tulinuia kumponya Babeli, lakini hajaponywa, haya na tumwache twende,
katika nchi yetu. Maana hatia yake imefika juu mbinguni; imerundikwa kufika
mawinguni. 10 Yahwe ametamka kwamba sisi hatuna hatia. Njooni, teseme katika

Sayuni matendo ya Yahwe Mungu wetu.' 11 Noweni mishale na kuchukua ngao.
Yahwe anaiimiza roho ya mfalme wa Umedi katika mpango wa kuiangamiza Babeli.
Hii ni kwa kisasi cha Yahwe, kisasi kwa maangamizi ya hekalu lake. 12 Inueni bendela
juu ya kuta za Babeli; wekeni walinzi. Wekeni waangalizi; wekeni askari waviziao
ili kumkamata kila akimbiliaye mjini, maana Yahwe atafanya kile alichokipanga.
Atafanya alichokisema juu ya wakaao Babeli. 13 Enyi mwishio kati ya chemchemi
nyingi za maji, ninyi mlio na wingi wa hazina, mwisho wenu umefika. upindo
wa maisha yenu umepunguzwa. 14 Yahwe wa majeshi ameapa kwa maisha yake,
'nitakujaza na adui zako, kama pigo la nzige; watainua kelele za vita juu yako.'
15 Ameifanya dunia kwa nguvu zake; akaiweka dunia mahali kwa hekima yake. Kwa
ufahamu wake alizitanda mbingu. 16 Anapovuma, kunakuwa na mvumo wa maji
mbinguni, maana huleta umande kutoka miisho ya dunia. Hufanya radi kwa ajili
ya mvua na kuituma na kuutuma upepo kutoka katika maghala ya nyumba zake.
17 Kila mtu anakuwa kama mnyama asiye na akili; kila mfua chuma ameaibishwa na
sanamu zake. Maana mwonekano wake unadanganya; maana hakuna uzima ndani
yake. 18 Hazifai, kazi ya wafanya mzaa; wataangamizwa wakati wa kuadhibiwa
kwao. 19 Lakini Mungu, urithi wa Yakobo, siyo kama hawa, maana yeye ndiye
afanyaye vitu vyote. Israeli ni kabila ya urithi wake; Yahwe wa majeshi ni jina lake.
20 Wewe ni nyundo ya vita yao, silaha ya vita yangu. Kwa wewe nitawaponda mataifa
na kuharibu falme. 21 Kwa wewe nitaponda farasi na wawapandao; kwa wewe
nitaponda vibandawazi na madereva wake. 22 Kwa wewe nitawafutilia mbali mme na
mke; kwa wewe nitafutilia mbali mzee na kijana. Kwa wewe nitafutilia mbali kijana
wa kiume na wasichana bikra. 23 Kwa wewe nitafutilia mbali wachungaji na makundi
yao; kwa wewe nitawafutilia mbali wakulima na jozi zao za kulimia. kwa wewe
nitawafutilia mbali watawala na maafsa. 24 Maana mbele yako nitamlipa Babeli na
wote wakaao Ukaldayo kwa maovu yote waliyoyafanya huko Sayuni - hili ni tamko
la Yahwe. 25 Tazama, mimi ni kinyume chako, ewe mlima, wewe unayewaharibu
watu wengine - hili ni tamko la Yahwe - kuiharibu dunia yote. Nitakupiga na
mikono yangu na kuvingirisha chini kutoka ukingo wa kilima. Kisha nitakufanya
mlima ulioteketezwa kabisa kwa moto. 26 Hivyo hawatachukua kwako jiwe lolote
ili kujengea pembe ya nyumba au msingi; kwani utakuwa ukiwa wa milele - hili ni
tamko la Yahwe. 27 Inua bendela ya vita juu ya nchi. Piga tarumbeta katika mataifa.
Yaite mataifa yamshambuliye: Ararati, Mini na Ashkenazi. Teua majemedari wa
kumshambulia; leta farasi kama nzige warukao. 28 Waandae mataifa kumshambulia:
wafalme wa Umedi na magavana wao, maafsa wake wote na nchi yake yete.
29 Maana nchi itatikisika na kudhoofika, kwa kuwa mipango ya Yahwe inaendelea
juu ya Babeli, kuifanya nchi ya Babeli kuwa nchi isiyofaa mahali pasipo na mtu.
30 Maaskari wameacha kupigana huko Babeli; wamekaa katika ngome zao. Nguvu
zao zimeshindwa; wamekuwa wanawake - nyumba zake zipo motoni, makomeo ya
malango yake yamevunjika. 31 Mjumbe hukimbia ili amwambie mjumbe mwingine,
na mtoa habari humwambia mtoa habari mwingine ili amwambie mfalme wa Babeli
kwamba mji wake umetwaliwa kutoka mwisho hata mwisho. 32 Hivyo vivuko katika
mito vimekamatwa; adui anaunguza mafunjo ya bwawa, na wapiganaji wa Babeli
wamechanganyikiwa. 33 Maana Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli, asema hivi:
Binti Babeli ni kama sakafu ya kupuria. Ni muda wa kumkanyaga. Ni kitambo
kidogo wakati wa mavuno utakuja juu yake. 34 Yerusalemu husema, 'Nebukadneza
mfalme wa Babeli amenirarua. Amenikausha na amenifanya kuwa mtungi mtupu.
Amenimeza kama joka. Alijishibisha kwa chakula changu chema. Amenitupa mbali.'
35 Wenyeji wa Sayuni watasema, 'Gasia nilizofanyiwa na mwili wangu na ziwe
kwa Babeli.' Yerusalem atasema, Damu yangu na iwe juu ya wakaao Ukaldayo.'

36 Kwa hiyo Yahwe asema hivi: Tazama, nikotayari kulitetea shitaka lako na kuleta
kisasi kwa ajili yako. Maana nitayakausha maji ya Babeli na kufanya vyanzo vyake
kukauka. 37 Babeli utakuwa rundo la magofu, pango la mbwea, sehemu itishayo, kitu
cha kutoa sauti ya nyoka, pasipo na watu. 38 Wababeli wataunguruma kwa pamoja
kama wanasimba. Watanguruma kama watoto wa simba. 39 wanapopashwa moto
kwa hasira, nitawafanyia sherehe; nitawalewesha hata wafurahi, na kisha kulala
usingizi usio na mwisho hata wasiamke - hili ni tamko la Yahwe - 40 nitawapeleka
chini kama wanakondoo kwa mchinjaji, kama kondoo dume pamoja na mbuzi majike.
41 Jinsi Babeli ulivyotekwa! Hivyo fahari ya dunia yote imekamatwa. Jinsi Babeli
ulivyofanyika sehemu yenye magofu kati ya mataifa. 42 Bahari imekuja juu ya Babeli!
Amefunikwa na mawimbi yavumayo. 43 Miji yake imekuwa ukiwa, sehemu kame na
nyika, nchi isiyo na watu, na hakuna mtu apitaye hapo. 44 Hivyo nitamwadhibu Beli
huko Babeli; nitakitoa kinywani mwake alichokimeza, na mataifa hawatamminikia
tena pamoja na wazao wao. Kuta za Babeli zitaanguka. 45 Tokeni kati yake, enyi
watu wangu. Kila mmoja wenu aokowe maisha yake kutoka katika hasira ya
gadhabu yangu. 46 Msiache mioyo yenu ikaogopa au kuhofu habari iliyosikiwa
nchini, maana habari itakuja siku moja. Baada yake mwaka unaofuata kutakuwa
na habari, na ghasia zitakuwa nchini. Mtawala atakuwa kinyume cha mtawala.
47 Kwa hiyo, tazama, siku zinakuja nitakapoadhibu sanamu za Babeli. Nchi yake
yote itaaibika, na wote waliochinjwa wataanguka ndani yake. 48 Kisha mbingu na
nchi, na vyote vilivyomo ndani yake vitafurahi juu ya Babeli. Maana mwalibifu
atamwijia kutoka kaskazini - hili ni tamko la Yahwe. 49 "Kama Babeli alivyowafanya
waliouawa wa Israeli kuanguka, hivyo waliouawa katika nchi yake wataanguka
katika Babeli. 50 Ondokeni!, manusura wa vita, Msikawiye. Mkumbukeni Yahwe
tokea mbali; Yerusalemu na ikumbukwe. 51 Tumeaibika, maana tumesikia matusi;
dhihaka imefunika nyuso zetu, maana wageni wameingia mahali patakatifu pa
nyumba ya Yahwe. 52 Kwa hiyo, tazama, siku zinakuja - hivi ndivyo asemavyo Yahwe
- nitakapoziadhibu sanamu zake, na waliojeruhiwa watanung'unika kwa maumivu
katika nchi yake yote. 53 Maana hata kama Babeli angepanda mbinguni au kujenga
ngome zake ndefu, aharibuye kutoka kwangu angemwendea - hili ni tamko la Yahwe.
54 Kelele ya maangamizi ilitoka Babeli, anguko kubwa kutoka nchi ya Wakaldayo.
55 Maana Yahwe anaiharibu Babeli. Anaifanya kelele ya sauti yake kuisha. Adui
zake wanaunguruma kama mawimbi ya maji mengi; kelele yao imekuwa na nguvu.
56 Maana aharibuye amekuja kinyume chake - kinyume cha Babeli! - na shujaa wake
wametekwa. Pinde zao zimevunjwa, maana Yahwe ni Mungu wa kisasi; atatekeleza
kisasi hiki. 57 Maana nitawafanya wana wafalme wake, wenye hekima wake, maofsa
wake, na maaskari wake kulewa, nao watalala usingizi kwa usingizi usioisha na bila
kuamka - hili ni tamko la mfalme: Yahwe wa majeshi ndilo jina lake. 58 Yahwe
wa majeshi asema hivi: Ukuta mnene wa Babeli utaangushwa kabisa, na malango
marefu yataunguzwa. Kisha watu wanaokuja kumsaidia watafanya kazi isiyofaa;
kila mataifa wanachojaribu kikifanya kwa ajili yake kitateketezwa kwa moto." 59 Hili
ndilo neno Yeremia nabii alilomwamru Seraya mwana wa Neria mwana wa Makseya
alipokwenda na Sedekia mfalme wa Yuda huko Babeli katika mwaka wa nne wa
kutawala kwake. Basi Seraya alikuwa afsa mwandamizi. 60 Maana Yeremia alikuwa
ameandika katika gombo kuhusu madhara yote yeliyokuwa yakienda kutendeka juu
ya Babeli - maneno haya yote yaliyokuwa yameandikwa juu ya Babeli 61 Yeremia
akamwambia Seraya, "Unapokwenda Babeli, hakikisha unayasoma maneno haya
yote. 62 Nawe utasema, 'Yahwe, wewe! - wewe mwenyewe umesema kwamba
utapaharibu mahali hapa. Hapatakuwa na wa kukaa, kwamba ni watu au wanyama.
Patakuwa nchi isiyofaa daima.' 63 Kisha mtakapomaliza kusoma gombo hili, funga

jiwe kubwa juu yake na ulitupe katikati ya Frati. [64] Sema, 'Babeli utazama kama
hivi. Hautainuka kwa sababu ya mabaya ninayoyapeleka juu yake, nao wataanguka."
Maneno ya Yeremia yanaishia hapa.

# 52

[1] Sedekia alikuwa na umri wa miaka ishirini na mmoja alipoanza kutawala;
akatawala miaka kumi na mmoja huko Yerusalemu. Jina la mamaye lilikuwa
Hamutali; alikuwa binti Yeremia wa Libna. [2] Akafanya maovu machoni pa Yahwe;
akafanya kila alichokifanya Yehoyakimu. [3] Kwa hasira ya Yahwe, matukio haya
yote yalitukia Yerusalemu na Yuda, hata alipowatoa mbele yake mwenyewe. Kisha
Sedekia akaasi dhidi ya mfalme wa Babeli. [4] Ikawa katika mwaka wa tisa wa
utawala wa mfalme Sedeki, katika mwezi wa kumi, na siku ya kumi ya mwezi
huo, Nebukadneza, mfalme wa Babeli, alikuja na jeshi lake lote dhidi ya Yerusalem.
Wakapiga kambi kuukabili, nao wakajenga ukuta wa kuusuria kuuzunguka. [5] Hivyo
mji ukausuriwa mpaka mwaka wa kumi na moja wa utawala wa mfalme Sedekia.
[6] Katika mwezi wa nne, siku ya tisa ya mwaka huo, njaa ikawa kali sana mjini hata
hakukuwa na chakula kwa watu wa nchi. [7] Kisha mji ukatobolewa, na wapiganaji
wote wakakimbia nje ya mji wakati wa usiku kwa njia ya lango lililokuwa kati ya
kuta mbili, kwa bustani ya mfalme, japokuwa Wakaldayo walikuwa wameuzunguka
mji. Hivyo wakaenda kwa njia ya Araba. [8] Lakini jeshi la Wakaldayo likamfuatia
mfalme na kumpata Sedekia katika tambarare za bonde la Mto Yordani karibu na
Yeriko. Jeshi lote lilikuwa limetawanyika mbali naye. [9] Wakamkamata mfalme na
kumleta hadi kwa mfalme wa Babeli huko Ribla katika nchi ya Hamathi, alipotoa
hukumu juu yake. [10] Mfalme wa Babeli akawachinja wana wa Sedekia mbele ya
macho yake, na huko Ribla akawachinja viongozi wote wa Yuda. [11] Kisha akayaondoa
macho ya Sedekia, akamfunga katika vifungo vya shaba, na kumleta Babeli. Mfalme
wa Babeli akamweka kifungoni hata siku ya kufa kwake. [12] Basi mwezi wa tano,
siku ya kumi ya mwezi, ambao ulikuwa mwaka wa kumi na tisa wa utawala wa
mfalme Nebukadneza, mfalme wa Babeli, Nebuzaradani akaja Yerusalemu. Alikuwa
jemedari wa walinzi wa mfalme na mtumishi wa mfalme wa Babeli. [13] Akaiteketeza
nyumba ya Yahwe, kasiri, na nyumba zote za Yerusalemu; pia kila jengo mhimu mjini
alilichoma. [14] Kama kwa kuta za kuuzunguka Yerusalemu, jeshi lote la Wababeli
lililokuwa pamoja na jemedari wa mlinzi wakaviaribu. [15] Kama kwa watu maskini
sana, watu waliosalia walioachwa katika mji, waliokuwa wamemwendea mfalme
wa Babeli, na baadhi ya watu wenye ujuzi - Nebuzaradan, jemedari wa askari
walinzi, akawachukua baadhi yao uhamishoni. [16] Lakini Nebuzaradani, jemedari wa
mlinzi, akawaacha baadhi ya maskini sana wa nchi kuitunza mizabibu na mashamba.
[17] Lakini kwa nguzo za shaba lilizokuwa katika nyumba ya Yahwe, mishikio na
bahari ya shaba iliyokuwa katika nyumba ya Yahwe, Wakaldayo wakaivunja vipande
wakaondoka navyo kurudi Babeli. [18] Vyungu, makoleo, kinara cha taa, mabakuri,
na vitu vyote vya shaba ambavyo makuhani walikuwa wakivitumia hekaluni -
Wakaldayo wakavichukua vyote. [19] Makalai na chetezo cha uvumba, mabakuri,
vyungu, kinara cha taa, vikaango, makalai zilizotengenezwa kwa dhahabu, na
zilizotengenezwa kwa dhahabu - kapteni wa mlinzi wa mfalme akazichukua pia.
[20] Nguzo mbili, bahari, na ng'ombe kumi na wawili wa shaba waliokuwa chini yake,
vitu Selemani alivyokuwa amevifanya kwa ajili ya nyumba ya Yahwe, vikiwa na
shaba nyingi sana isiyoweza kupimwa. [21] Nguzo zilikuwa na urefu wa dhiraha
kumi na nane kila moja, na mstari kuzunguka kila moja wenye urefu wa dhiraha
kumi na mbili. Kila moja ilikuwa na unene wa vidole vinne na tundu. [22] Kichwa
cha shaba kilikuwa juu yake. Kichwa kilikuwa dhiraha tano urefu wake, kazi ya

waya zinazokingamana na makomamanga kukizunguka. Chote kilitengenezwa kwa
shaba. Na nguzo nyingine ilikuwa na makomamanga yake vilikuwa kama ya kwanza.
23 Hivyo kulikuwa na makomamanga tisini na sita ubavuni mwa kila kichwa, na
makomamanga mia moja juu ya nyaya zilizokingamana kukizunguka. 24 Jemedari
wa mlinzi akamchukua Seraya mfungwa, kuhani mkuu, pamoja na Sefania, kuhani
wa pili, na wale mabawaba watatu. 25 Kutoka mjini akamchukua mfungwa afsa
aliyekuwa juu ya askari, na watu saba wa wale waliomshauri mfalme, waliokuwa
wamesalia mjini. Akamchukua mfungwa afsa wa jeshi la mfalme aliyekuwa na
wajibu wa kuwaingiza watu katika jeshi, pamoja na watu mashuhuri sitini kutoka
katika nchi waliokuwamo mjini. 26 Kisha Nebuzaradani, jemedari wa mlinzi,
akawachukuwa na kuwaleta kwa mfalme wa Babeli huko Ribla. 27 Mfalme wa
Babeli akawaua huko Ribla katika nchi ya Hamathi. Kwa njia hii, Yuda akaondoka
katika nchi yake na kwenda uhamishoni. 28 Hawa walikuwa watu Nebukadneza
aliwaamisha: katika mwaka wa saba, Wayudea 3, 023. 29 Katika mwaka wa kumi
na nane wa Nebukadneza alichukuwa 832 kutoka Yerusalemu. 30 Katika mwaka wa
ishirini na tatu wa Nebukadneza, Nebuzaradani, jemedari wa walinzi wa mfalme,
aliwahamisha Wayudea 745. Jumla ya watu walioamishwa walikuwa 4, 600. 31 Ikawa
baadaye katika mwaka wa thelathini na saba wa kufungwa kwake Yohoyakini,
mfalme wa Yuda, katika mwezi wa kumi na mbili, siku ya ishirini na tano ya mwezi,
Evili Merodaki, mfalme wa Babeli akamfungua Yehoyakini mfalme wa Yuda kutoka
kifungoni. Ilikuwa mwaka ambao Evili Merodaki alianza kutawala. 32 Akaongea naye
kwa upole na akampa kiti cha heshima kuliko cha wafalme wengine aliokuwa pamoja
nao huko Babeli. 33 Evili Merodaki akaondoa mavazi ya gerezani ya Yehoyakini, na
Yehoyakini akala chakula cha daima katika meza ya mfalme siku zote zilizosalia za
maisha yake. 34 Na alipewa posho ya chakula cha kila siku kwa maisha yake yote
yaliyosalia mpaka siku ya kufa kwake.

# Maombolezo

[1] Mji ambao mwanzo ulikuwa na watu wengi sasa umekaa peke yake. Amekuwa
kama mjane, japo alikuwa taifa kubwa. Alikuwa mtoto wa mfalme miongoni mwa
mataifa, lakini sasa amelazimishwa utumwani. [2] Analia na kuomboleza usiku, na
machozi yake yanafunika mashavu yake. Hamna ata mpenzi wake anaye mliwaza.
Marafiki wake wote wamemsaliti. wamekuwa maadui wake. [3] Baada ya umaskini
na mateso, Yuda ameenda matekani. Anaishi miongoni mwa mataifa na hapati
pumziko lolote. Wanao wakimbiza wamewapata katika upweke wake. [4] Barabara za
Sayuni zinaomboleza kwasababu hakuna anaye kuja kwenye sherehe iliyo andaliwa.
Malango yake yote ni ukiwa. Makuhani wake wote wana sononeka. Mabikra wake
wana uzuni na yeye mwenyewe yupo katika ugumu. [5] Maadui wake wamekuwa
bwana zake; maadui wake wana fanikiwa. Yahweh amemuadhibu kwa dhambi
zake nyingi. Watoto wake wadogo wanaenda matekani kwa maadui zake. [6] Uzuri
umemwacha binti wa Sayuni. Watoto wa mfalme wamekuwa kama ayala ambaye
haoni malisho, na wanaenda bila uwezo kwa wanao wakimbiza. [7] Katika siku
za mateso yake na kutokuwa na nyumba, Yerusalemu itakumbuka hazina zake
za dhamani alizo kuwa nazo awali. Wakati watu wake walipo angukia mikononi
mwa adui, hakuna aliye msaidia. Maadui waliwaona na kucheka maangamizo
yake. [8] Yerusalemu ili tenda dhambi sana, hivyo basi, amedhalillika kama kitu
kichafu. Wote walio mheshimu sasa wana mdharau kwa kuwa wameona uchi
wake. Anasononeka na kujaribu kugeuka pembeni. [9] Amekuwa mchafu chini ya
sketi yake. Hakuwaza hatima yake. Anguko lake lilikuwa baya. Hakukuwa na
wakumliwaza. Alilia, “Angalia mateso yangu, Yahweh, kwa kuwa adui amekuwa
mkuu sana.” [10] Adui ameeka mkono wake kwenye hazina zetu za dhamani. Ameona
mataifa yakiingia sehemu yake takatifu, japo uliamuru wasiingie katika sehemu yako
ya kukusanyikia. [11] Watu wote wana sononeka wanapo tafuta mkate. Wametoa
hazina zao za dhamani kwa ajili ya chakula cha kurejesha uhai wao. Tazama,
Yahweh, ni kumbuke mimi, kwa kuwa nimekuwa sina faida. [12] Sio kitu kwako, wote
mnao pita? Angalia na uone kama kuna mtu mwenye uzuni kama uzuni ninao
teswa nao, tangu Yahweh amenitesa mimi katika siku ya hasira yake kali. [13] Ni
kutoka juu ndipo alipo tuma moto kwenye mifupa yangu na umenishinda. Ametanda
nyavu kwa miguu yangu na kunigeuza. Amenifanya ukiwa na dhahifu. [14] Nira
ya makosa yangu imefungwa na mikono yake. Zimesokotwa na kuekwa shingoni
mwangu. Amefanya uweza wangu kushindwa. Bwana amenikabidhi mikononi
mwa, na siwezi kusimama. [15] Bwana ametupa pembeni wanaume wangu hodari
walio niokoa. Ameitisha kusanyiko dhidi yangu kuponda wanaume wangu imara.
Bwana amewakanyaga binti bikra wa Yuda kwenye chombo cha kusagia mvinyo.
[16] Kwa vitu hivi ninalia. Macho yangu, maji yanashuka chini ya macho yangu
tangu mfariji aliye paswa kurejesha maisha yangu yuko mbali na mimi. Watoto
wangu wamekuwa ukiwa kwasababu adui yangu ameshinda. [17] Sayuni ametandaza
mikono yake; hakuna wakuwa mliwaza. Yahweh ameamuru hao karibu na Yakobo
wawemaadui wake. Yerusalemu ni kitu kichafu kwao. [18] Yahweh ni mwenye haki,
kwa kuwa nimeasi dhidi ya amri zake. Sikia, ninyi watu, na muone uzuni wangu.
Mabikra wangu na wanaume imara wameenda matekani. [19] Niliita marafiki zangu,
lakini walikuwa na hila kwangu. Makuhani wangu na wazee waliangamia kwenye
mji, walipo kuwa wanatafuta chakula cha kurejesha uhai wao. [20] Tazama, Yahweh,
kwa kuwa nipo kwenye ugumu; tumbo langu lina nguruma, moyo wangu umetibuka
ndani yangu, kwa kuwa nimekuwa muasi sana. Nje, upanga umemliza mama, ndani

ya nyumba kuna mauti tu. 21 Wamesikia sononeko langu, lakini hakuna wakuni
liwaza. Maadui zangu wote wamesikia shida zangu na wamefurahi umenifanyia
hivi. Umeleta siku uliyo ahidi; sasa acha wawe kama mimi. 22 Acha uovu wote uje
mbele zako. Shughulika nao kama ulivyo shughulika na mimi kwasababu ya makosa
yangu yote. Masononeko yangu ni mengi na moyo umezimia.

# 2

1 Bwana amemfunika binti wa Sayuni chini ya wingu la hasira yake. Ametupa
utukufu wa Israeli chini kutoka mbinguni hadi duniani. Hajakumba stuli yake ya
miguu siku ya hasira yake. 2 Bwana amemeza na hajawa na huruma kwa miji yote
ya Yakobo. Siku za hasira zake ameangusha miji imara ya binti wa Yuda; kwa aibu
ameshusha chini ufalme na watala wake. 3 Kwa hasira kali amekata kila pembe ya
Israeli. Ameurudisha mkono wake kutoka kwa adui. Amechoma Yakobo kama moto
mkali unao teketeza kila kitu karibu yake. 4 Kama adui amepindisha upinde wake
kuelekea kwetu, na wakulia wake yupo tayari kushambulia. Amewachinja wote walio
kuwa wanampendeza katika hema la binti wa Sayuni; Amemwaga gadhabu yake
kama moto 5 Bwana amekuwa kama adui. Amemeza Israeli. Amemeza majumba
yake yote. Ameharibu ngome zake. Ameongeza kilio na maombolezo kati ya mabinti
wa Yuda. 6 Ameshambulia hema lake la kukutania kama kajumba cha bustani.
Ameharibu sehemu ya kukusanyikia. Yahweh amesababisha kukusanyika na Sabato
kusahaulika Sayuni, kwa kuwa amemdharau mfalme na kuhani katika ukali wa
hasira yake. 7 Bwana amekataa madhabahu yake na kukana sehemu yake takatifu.
Ametoa kuta za majumba mikononi mwa adui. Wamepaza sauti nyumbani mwa
Yahweh, kama siku ya sherehe. 8 Yahweh aliamua kuharibu ukuta wa mji wa binti
wa Sayuni. Amenyoosha kamba ya kipimo na hajauzuia mkono wake kutoharibu
ukuta. Amefanya minara na ukuta kuomboleza; pamoja vilipotea. 9 Malango
yake yameanguka chini, ameharibu na kuvunja chuma za ukuta. Mfalme wake
na watoto wa mfalme wapo miongoni mwa mataifa, sheria haipo tena na manabii
wake hawapati maono kutoka kwa Yahweh. 10 Wazee wa binti wa Sayuni wameketi
chini na ukimya. Wamerusha vumbi kichwani mwao na kuvaa magunia. Mabikra
wa Yerusalemu wameinamisha vichwa vyao chini. 11 Macho yangu yamekaukiwa
machozi yake; tumbo langu la nguruma; sehemu zangu za ndani zimemwagika chini
kwasababu ya uharibifu wa binti wa watu wangu, watoto na wachanga wamezimia
mitaani mwa mji. 12 Wanasema kwa mama zao, “Mbegu ziko wapi na mvinyo?” kama
wanavyo zimia kama mtu aliye jeruhiwa mitaani mwa mji, maisha yao yamemwaga
kwenye kifua cha mama zao. 13 Nini naeza kusema kwako, binti wa Yerusalemu?
Naweza kufananisha na nini, ili ni kufariji, binti bikra wa Sayuni? Jera lako ni
kubwa kama bahari. Nani anaweza kukuponya? 14 Manabii wako wameona uongo
na maono batili kwa ajili yako. Hawaja weka wazi dhambi zako kurejesha mali zako,
lakini kwako wametoa matamko ya uongo na ya kupotosha. 15 Wote wanao pita
pembeni mwa barabara wana piga makofi kwako. Wanaguna na kutikisa vichwa
vyao dhidi ya binti wa Yerusalemu na kusema, “Huu ndio mji walio uita 'Ukamilifu
wa uzuri,' 'Furaha ya Dunia Yote'?” 16 Maadui zako wote walifungua vinywa vyao
na kukudhihaki. Walizomea na kusaga meno na kusema, “Tumemmeza yeye! Hii
ni siku tulio subiri! Tumeishi kuweza kuiona!” 17 Yahweh amefanya alivyo panga
kufanya. Ametimiza neno lake. Amekupindua bila huruma, kwa kuwa amemruhusu
adui kukusherehekea; amenyanyua pembe za maadui zako. 18 Mioyo yao ikamlilia
Bwana, kuta za binti wa Sayuni! Fanya machozi yako kutiririka chini kama mto usiku
na mchana. Usijipatie hauweni, macho yako bila hauweni. 19 Nyanyuka, lia usiku,
mwanzo usiku wa manane! Mwaga moyo wako kama maji mbele za uso wa Bwana.

Nyoosha juu mikono yako kwa ajili ya uzima wa watoto wako wanao zimia kwa njaa
kwenye njia ya kila mtaa. 20 Ona, Yahweh, na ukumbuke hao ulio watende haya.
Wanawake wale tunda la uzazi wao, watoto walio wajali? Makuhani na manabii
wa chinjwe sehemu takatifu ya Bwana? 21 Wote wadogo kwa wakubwa wana keti
kwenye udongo wa mitaa. Wanawake wangu wadogo na wanaume wangu wadogo
wameanguaka kwa upanga; umewachinja pasipo kuwa hurumia. 22 Umeitisha, kama
ungewaita watu katika siku ya maakuli, hofu yangu kila sehemu, katika siku ya
hasira ya Yahweh hakuna aliye toroka; hao niliyo wajali na kuwakuza, adui wangu
amewaharibu.

# 3

1 Mimi ni mwanaume nilyeona maangaiko chini ya gongo la hasira ya Yahweh.
2 Amenifukuza na kunisababisha kutembea kwenye giza kuliko kwenye nuru.
3 Hakika amenigeuzia mkono wake dhidi yangu tena na tena, siku yote. 4 Amefanya
mwili wangu na ngozi yangu kufifia; amevunja mifupa yangu. 5 Amejenga vifusi
vya udogo dhidi yangu, na kunizingira na uchungu na ugumu. 6 Amefanya ni ishi
sehemu za giza, kama hao walio kufa zamani. 7 Amejenga ukuta kunizunguka
na siwezi kutoroka. Amefanya minyororo yangu mizito 8 na japo nina ita na
kulilia msaada, anazima maombi yangu. 9 Ameziba njia yangu kwa ukuta wa
mawe ya kuchonga; amefanya njia yangu mbaya. 10 Yeye ni kama dubu anasubiri
kunishambulia, simba katika maficho; 11 amegeuza pembeni njia zangu, amenifanya
ukiwa. 12 Amepindisha upinde wake na kunifanya mimi kama lengo la mshale wake.
13 Ametoboa maini yangu kwa mishale ya mfuko wake. 14 Nilikuwa kichekesho
kwa watu wangu wote, kielelezo cha dhihaka yao siku nzima. 15 Amenijaza kwa
uchungu na kunilazimisha kunywa maji machungu. 16 Alivunja meno yangu na
kokoto; amenisukuma chini kwenye fumbi. 17 Nafsi yangu imenyimwa amani;
nimesahau furaha ni nini. 18 Hivyo na sema, “Ustahimilivu wangu umeangamia na
pia tumaini langu kwa Yahweh.” 19 Kumbuka mateso yangu na kuangaika kwangu,
maji machungu na uchungu. 20 Ninaendelea kukumbuka na nimeinama ndani yangu.
21 Lakini ni vuta hili akilini mwangu na hivyo nina matumaini: 22 Upendo dhabiti
wa Yahweh haukomi na huruma zake haziishi, 23 ni mpya kila asubui; uaminifu
wako ni mkubwa. 24 “Yahweh ni urithi wangu,” Nilisema, hivyo nitamtumainia.
25 Yahweh ni mwema kwao wanao msubiri, kwa anaye mtafuta. 26 Ni vizuri kusubiri
taratibu kwa uwokovu wa Yahweh. 27 Ni vizuri kwa mtu kubeba nira katika ujana.
28 Acha aketi peke yake katika utulivu, inapo kuwa imewekwa juu yake. 29 Acha
aeke mdomo wake kwenye vumbi - kunaweza bado kuwa na matumaini. 30 Acha
atoa shavu lake kwa yeye anaye mpiga, na ajazwe tele kwa aibu. 31 Kwa kuwa
Bwana hatatukataa milele, 32 lakini japo anatia uzuni, ata kuwa na huruma kwa
kadiri ya mwingi wa upendo wake dhabiti. 33 Kwa kuwa haadhibu kutoka moyoni
mwake au kutesa watoto wa mwanadamu. 34 Kukanyaga chini ya mguu wafungwa
wote wa dunia, 35 kumnyima haki mtu mbele ya uwepo wa Aliye Juu, 36 mkunyima
haki mtu - Bwana hataidhinisha vitu kama hivyo! 37 Ni nani aliye zungumza na
ikatimia, kama sio Bwana kutamka? 38 Sio kutoka mdomoni mwa Aliye Juu majanga
na mazuri yanakuja? 39 Mtu aliye hai anawezaje kulalamika? Mtu anawezaje
kulalamika kwa adhabu ya dhambi zake? 40 Natujichunguze njia zetu na kuzijaribu,
na tumrudie Yahweh. 41 Na tunyanyue mioyo yetu na mikono yetu kwa Yahweh
mbinguni: 42 “Tumekosea na kuasi, na haujasamehe. 43 Umejifunika na hasira na
kutukimbiza, umeua na haujanusuru. 44 Umejifunika na wingu ili kwamba kusiwe
na ombi linaloweza kupita. 45 Umetufanya kama uchafu na taka miongoni mwa
mataifa. 46 Maadui wetu wote wametulaani, 47 wasiwasi na shimo limetujia, maafa

na uharibifu. 48 Macho yangu yanatiririka na miferiji ya machozi kwasababu ya watu
wangu. 49 Macho yangu yatatoa machozi pasipo kikomo; pasipo hauweni, 50 mpaka
atakapo tazama chini na Yahweh ataona kutoka mbinguni. 51 Macho yangu yana
ni sababishia uzuni kwasababu ya mabinti wa mji wangu. 52 Nimewindwa kama
ndege hao walio kuwa maadui zangu; wameniwinda pasipo sababu. 53 Wamenitupa
kwenye shimo na wakanitupia jiwe, 54 na maji yaka mwagika juu ya kichwa changu.
Nilisema, “Nimekatwa mbali!” 55 Nililiita jna lako, Yahweh, kutoka kina cha shimo.
56 Ulisikia sauti yangu. Ulisikia sauti yangu nilipo sema, “Usifunge sikio lako kwa
kilio changu cha msaada.” 57 Ulikuja karibu siku niliyo kuiita; ulisema, “Usiogope”
58 Bwana, ulitetea kesi yangu, uliokoa maisha yangu! 59 Yahweh, umeona mabaya
waliyo ni fanyia, hukumu kesi yangu. 60 Umeona matusi yao, mipango yao yote dhidi
yangu - 61 Umesikia dhihaka yao, Yahweh, na mipango yao kunihusu. 62 Midomo ya
hao wanao inuka kinyume changu, na mashtaka yao, inakuja dhidi yangu siku nzima.
63 Ngalia jinsi wanavyo keti na kuinuka; wana nidhihaki na nyimbo zao. 64 Walipize,
Yahweh, kwa kadiri ya waliyo fanya. 65 Utaacha mioyo yao bila lawama! Hukumu
yako iwe juu yao! 66 Una wakimbiza kwa hasira na kuwaharibu nchini ya mbingu,
Yahweh!

# 4

1 Dhahabu imechakaa; jinsi gani dhahabu safi imebadilika! Mawe matakatifu
yamezagaa katika kila njia ya mtaa. 2 Wana wa dhamani wa Sayuni walikuwa na
dhamani ya uzito wa dhahabu safi, lakini sasa hawana dhamani zaidi ya majagi
ya udogo, kazi ya mikono ya mfinyazi! 3 Ata mbwa wa mitaani wanatoa maziwa
yao kuwanyonyesha watoto wao, lakini binti wa watu wangu amekuwa katili, kama
mbuni katika jangwa. 4 Ulimi wa mtoto mchanga anaye nyonya unagota juu mdomo
wake kwa kiu; watoto wanaomba chakula, lakini hakuna kwa ajili yao. 5 Wao
walizoea kula chakula cha gharama sasa wana shinda njaa mitaani; wao walio
lelewa kwa kuvaa nguo za zambarau, sasa wamelala katika majalala. 6 Hukumu
ya binti wa watu wangu ni kubwa kuliko hiyo ya Sodoma, na ilipinduliwa kwa
dakika na hakuna aliye yanyua mkono kumsaidia. 7 Viongozi wake walikuwa
wasafi kuliko theluji, weupe kuliko maziwa; miili yao ilikuwa imara kuliko jiwe,
mwili wao ulikuwa kama yakuti samawi. 8 Muonekano wao umekuwa mweusi
kama giza; hawatambuliki mitaani. Ngozi zao zimesinya kwenye mifupa yao;
imekuwa kavu kama kuni. 9 Hao walio uawa kwa upanga walikuwa na furaha
zaidi kuliko hao walio kufa kwa njaa, walio potea, wakatobolewa kwa ukosefu wa
mavuno shambani. 10 Mikono ya wanawake wenye huruma imewachemsha watoto
wao; wamekuwa chakula chao wakati ambapo binti wa watu wangu alipo kuwa
akiharibiwa. 11 Yahweh alionyesha gadhabu yake yote; alimwaga hasira yake kali.
Aliwasha moto Sayuni uliteketeza misingi yake. 12 Wafalme wa dunia hawaku amini,
wala wakazi wa dunia, kwamba maadui au wapinzani waliweza kuingia malangoni
ya Yerusalemu. 13 Haya yalitokea kwasababu ya dhambi za manabii na na maasi
ya makuhani walio mwaga damu ya wenye haki mbele zake. 14 Walitanga, kwa
upofu, mitaani. Walikuwa wamejitia unajisi kwa damu hiyo ambapo hakuna aliye
ruhusiwa kushika nguo zao. 15 “Kaa mbali! Wewe mnajisi!” Watu waliwapazia sauti.
“Kaa mbali! Kaa mbali! Usiguse!” Hivyo wakatanga; watu walisema miongoni mwa
mataifa, “Hawawezi kukaa hapa tena.” 16 Yahweh mwenyewe akawatawanyisha;
hawatazami tena. Hawa waheshimu makuhani, na hawaonyeshi upendeleo kwa
wazee. 17 Macho yetu yalikwama, yakitazama bure kwa msaada; kutoka minara yetu
ya ulinzi tulitazama taifa lisilo weza tuokoa. 18 Walifuata hatua zetu, hatukuweza
kutembea mitaani mwetu. Mwisho wetu ulikuwa karibu na siku zetu zilihesabiwa,

mwisho wetu ulifika. [19] Walio tukimbiza walikuwa wepesi kuliko tai wa aangani.
Walitukimbiza kwenye milima na kutuwinda nyikani. [20] Pumzi katika pua zetu -
mpakwa mafuta wa Yahweh - ndiye aliye kamatwa katika shimo; ambaye ndiye aliye
semewa, "Chini ya kivuli chake tutaishi miongoni mwa mataifa." [21] Shangilia na
ufurahi, binti wa Edomu, wewe unaye ishi nchi ya Uzi. Lakini kwako pia kikombe
kitapitishwa; utalewa na kuvua nguo. [22] Binti wa Sayuni, hukumu yako itafika
mwisho, hataongeza mateka yako lakini binti wa Edomu, ata muhadhibu; ata funua
dhambi zako.

# 5

[1] Kumbuka, Yahweh, yaliyo tutokea na uone aibu yetu. [2] Urithi wetu umegeuziwa
kwa wageni; nyumba zetu kwa wageni. [3] Tumekuwa yatima, bila baba, na mama
zetu ni kama wajane. [4] Lazima tulipe fedha kwa maji tunayo kunywa, na tulipe fedha
kupata mbao zetu. [5] Hao wanakuja kwetu wamekaribia nyuma yetu; tumechoka na
hatuwezi pata mapumziko. [6] Tumejitoa kwa Misri na kwa Assiria tupate chakula cha
kutosha. [7] Baba zetu walifanya dhambi, na hawapo tena, na tumebeba dhambi zao.
[8] Watumwa walitutawala, na hakuna wa kutuokoa na mikono yao. [9] Tunapata mkate
wetu pale tunapo hatarisha maisha, kwasababu ya upanga wa nyikani. [10] Ngozi zetu
zimekuwa na moto kama jiko kwasababu ya joto la njaa. [11] Wanawake wanabakwa
Sayuni, na mabikra katika mji wa Yuda. [12] Watoto wa mfalme wamenyongwa na
mikono yao, na hakuna heshima inayoonyeshwa kwa wazee. [13] Wanaume vijana
wanalizimishwa kusaga mbegu kwa jiwe la kusagia, na wavulana wanajikwa chini
ya vifurushi vya kuni. [14] Wazee wameacha lango la mji, na vijana wameacha miziki.
[15] Furaha ya moyo imekoma na kucheza kwetu kumegeuka kilio. [16] Taji limeanguka
kichwani mwetu; ole wetu, kwa kuwa tumetenda dhambi! [17] Kwa kuwa moyo wetu
umekuwa unaumwa, na machozi yetu ya fifia, kwa vitu hivi macho yetu yanafifia
[18] maana Mlima Sayuni umelala ukiwa, mbwa wa mitaani wacheza juu yake. [19] Lakini
wewe, Yahweh, unatawala milele, na utaketi katika kiti chako cha enzi vizazi na
vizazi. Kwanini unatusahau milele? [20] Kwanini unatutelekeza kwa siku nyingi?
[21] Turejeshe kwako, Yahweh, na sisi tutarejea. Fanya upya siku zetu kama zilivyo
kuwa hapo zamani - [22] vinginevyo labda uwe umetukataa na una hasira kwetu kupita
kiasi.

# Ezekieli

[1] Katika mwaka wa thelathini, mwezi wa nne, na siku ya tano ya mwezi, ikawa
kuhusu kwamba nilikuwa nikiishi miongoni mwa wafungwa karibu na Kebari Kanali.
Mbingu zilifunguka, na kuona maono ya Mungu. [2] Katika siku ya tano katika mwezi
huo-ilikuwa mwaka wa tano wa utumwani wa Mfalme Yehoyakini- [3] Neno la Yahwe
likamjia Ezekieli mwana wa Buzi kuhani, katika nchi ya Wakaldayo karibu na Keberi
Kanali, na mkono wa Yahwe ulikuwa juu yake hapo. [4] Kisha nikaona, kulikuwa na
upepo wa dhoruba unakuja kutoka kaskazini; wingu kubwa pamoja na moto wa
nuru ndani yake na kung'aa ukizunguka ndani yake, na moto ulikuwa na rangi ya
kaharabu ndani ya hilo wingu. [5] Katikati kulikuwa na viumbe vinne vinavyofanana.
Mwonekano wao ulikuwa hivi: walikuwa wanamfanano wa mtu, [6] lakini walikuwa
na sura nne kila mmoja, na kila mmoja alikuwa na mabawa manne. [7] Miguu yao
ilikuwa imenyooka, lakini nyayo za miguu yao zilikuwa kama kwato za ndama
zilizokuwa zinang'aa kama shaba iliyosuguliwa. [8] Bado walikuwa na mikono ya
binadamu chini ya mabawa yao chini kwenye pande zote nne. Kwa wote wanne,
nyuso zao na mabawa vilikuwa hivi: [9] mabawa yao yalikuwa yameungana na kiumbe
kingine, na hawakurudi walipokuwa wameenda; badala yake, kila mmoja alienda
mbele. [10] Mfanano wa nyuso zao ulikuwa kama uso wa mwanadamu. Wanne hao
walikuwa na uso wa simba kwa upande wa kuume. Hao wanne pia walikuwa na uso
wa tai. [11] Nyuso zao zilikuwa hivyo, na mabawa yao yalikuwa yametawanyika juu,
hivyo basi kila kiumbe kilikuwa na jozi ya za mabawa yaliyokuwa yameshikamana
na bawa la kiumbe kingine, na pia jozi za mabawa yaliyokuwa yamefunika miili
yao. [12] Kila mmoja aliendа mbele, hivyo basi popote Roho alipowaelekeza kwanda,
walienda bila kurudi. [13] Kama kwa mfanano wa hao viumbe hai, mwonekano
wao ulikuwa ni kama kuchoma kaa la moto, kama mwonekano wa nuru; mng'ao
wa moto pia ulihama karibu na miongoni mwa viumbe, na kulikuwa na nuru za
radi. [14] Hao viumbe hai vilikuwa vikihama mbio mbele na nyuma, na walikuwa
na mwonekano wa radi! [15] Kisha nikawatazama wale viumbe hai; kulikuwa na
gurudumu moja juu ya aridhi kando ya vile viumbe hai. [16] Huu ndio ulikuwa
mwonekano na umbo wa hizo gurudumu: kila gurudumu lilikuwa kama zabarajadi,
na manne hayo yalikuwa na mfano mmoja; mwonekano wao na umbo vilikuwa
kama gurudumu lililoungana na jingine. [17] Wakati yale magurudumu yalipokuwa
yakitembea, yalienda bila kurudi kwenye mwelekeo wowote viumbe vilipokuwa
vimeelekea. [18] Kama kwa upande kingo, walikuwa warefu na wakutisha, kwa
upande kingo kulikuwa na macho yamezunguka kote. [19] Popote vile viumbe hai
vilipokuwa vikielekea, yale magurudumu yalielekea karibu nao. Wakati vile viumbe
hai vilipoinuka kutoka kwenye nchi, na yale magurudumu yaliinuka pia. [20] Popote
Roho alipokwenda, walikwenda, na yale magurudumu yaliinuka karibu nao, roho wa
kiumbe hai ilikuwa magurudumu. [21] Popote vile viumbe vilipoelekea, magurudumu
pia yalielekea huko; na wakati wale viumbe viliposimama hata hivyo, magurudumu
yalisimama bado; wakati viumbe viliposimama kutoka kwenye nchi, magurudumu
yalisimama karibu nao, kwa sababu yule roho wa wale viumbe alikuwa kwenye
magurudumu. [22] Juu ya vichwa vya wale viumbe hai kulikuwa na mfanano wa anga
la kutanuka; ilikuwa inang'aa kama mfano wa barafu juu ya vichwa vyao. [23] Chini ya
anga, kila mabawa ya kiumbe kimoja yalinyooshwa mbele na kugusana kila mabawa
na kiumbe kimoja. Pia kila kiumbe hai kilikuwa na jozi moja kwa ajili ya kujifunika
vyenyewe; kila kimoja kilikuwa na jozi moja kwa ajili ya kujifunika mwili wake

mwenyewe. 24 Kisha nikasikia sauti ya mabawa yao. Kama mlio wa maji mengi.
Kama sauti ya mwenye enzi popote walipoelekea. Kama sauti ya jeshi. Popote pale
waliposimama, walishusha mabawa yao. 25 Sauti ikaja kutoka juu ya anga juu ya
vichwa vyao popote waliposimama na kushusha mabawa yao. 26 Juu ya anga juu ya
vichwa vyao kulikuwa na mfanao wa kiti cha enzi ambacho kilikuwa na mwonekano
wa jiwe la samawati, na juu mfano wa kiti cha enzi kilifanana kama mwonekano
wa mwanadamu. 27 Nikaona umbo lenye mwonekano wa chuma chenye kung'aa
pamoja na moto ndani yake kutoka kwenye mwonekano wa juu ya nyonga zake juu;
Nikaona kutoka kwenye mwonekano wa nyonga zake upande wa chini mwonekano
wa moto na mng'ao umezunguka kote. 28 Kama mwonekano wa upinde wa mvua
kwenye mawingu katika siku ya mvua ulikuwa na mwonekano wa taa iliyowaka
imeizunguka. ulikuwa na mwonekano unaofanana na utukufu wa Yahwe. Wakati
nilipouona, nilihisi kwenye uso wangu, na nikasikia sauti ikiongea.

## 2

1 Akanambia, “Mwana wa adamu, simama kwa miguu yako; kisha nitaongea
na wewe.” 2 Kisha, alipokuwa akiongea na mimi, Roho akaingia ndani yangu na
ikaniweka kwenye miguu yangu, na nikamsikia akiongea na mimi. 3 Akanambia,
“Mwana wa adamu, nakutuma kwa watu wa Israeli, kwa mataifa yanayoasi ambayo
yameasi dhidi yangu-wote wao na babu zao wameasi juu yangu hata hivi leo!
4 Vizazi vyao vina sura za kikaidi na mioyo migumu. Nakutuma wewe kwenda
kwao, na utawaambia, 'Hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo.' 5 Labda watasikia
au hawatasikia. Ni nyumba za uasi, lakini angalau watajua kwamba nabii alikuwa
miongoni mwao. 6 Wewe, mwanadamu, usiwaogope au maneno yao. Usiogope,
ingawa utakuwa pamoja na mitemba na miiba na ijapokuwa unaishi na nge.
Usiogope maneno yao au kuvunjika moyo kwa nyuso zao, kwa kuwa ni nyumba zenye
kuasi.. 7 Lakini utawaambia maneno yangu, labda watasikia au hapana, kwa sababu
ni waasi mno. 8 Lakini wewe, mwanadamu, silikiliza kile nisemacho kwako. Usiwe
muasi kama nyumba za uasi. Fungua mdomo wako na ule kile ninachotaka kukupa!”
9 Kisha nikaona, na mkono ulikuwa umenyooshwa kwangu; ndani yake kulikuwa na
hati ya kukunja. 10 Akaikinjua mbele yangu; ilikuwa imeandikwa pande zote mbele
na nyuma, na yalikuwa yameandikwa maombolezo kwenye hiyo hati ya kukunja, na
huzuni, na ole.

## 3

1 Akanambia, “Mwanadamu, kile ulichokikuta, kula. Kula hili gombo, kisha nenda
kaongee na nyumba ya Israeli.” 2 Basi nikafungua kinywa changu, na akanilisha hilo
gombo. 3 Akanambia, “Mwana wa adamu, lisha tumbo lako na jaza tumbo lako kwa
hili gombo ambalo nimekupa!” Basi nikalila, na lilikuwa tamu kama asali kwenye
mdomo wangu. 4 Kisha akanambia, “Mwana wa adamu, nenda kwenye nyumba
ya Israeli na ongea maneno yangu kwao. 5 Kwa kuwa hujatumwa kwa watu wenye
maneno ya kushangaza au lugha ngumu, lakini kwa nyumba ya Israeli- 6 sio kwa taifa
lenye nguvu ya maneno ya ajabu au lugha ngumu ambao maneno yao hutaweza
kuyaelewa! Kama nikikutuma kwao, watakusikiliza. 7 Lakini nyumba ya Israeli
haitakuwa tayari kukusikiliza, kwa kuwa hawako tayari kunisikiliza mimi. Hivyo
nyumba yote ya Israeli ni paji gumu na moyo mgumu. 8 Kumbe nimeufanya uso wako
kama kaidi kama nyuso zao na paji lako kuwa gumu kama mapaji yao. 9 Nimekufanya
paji lako kama almasi, gumu kuliko jiwe la kiberiti! Usiwaogope wala kufadhaika kwa
nyuso zao, kwa kuwa ni nyumba ya uasi.” 10 Kisha akanambia, “Mwana wa adamu,
maneno yote niliyokutangazia-yachukue kwenye moyo wako na wasikize kwa sikio

lako! 11 Kisha nenda kwa watumwa, kwa watu wako, na uzungumze nao. Waambie,
'Hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo; iwapo watasikia au hapana." 12 Kisha Roho
akaniinua juu, na nikasikia nyuma yangu sauti yenye tetemeko la aridhi: "Ubarikiwe
utukufu wa Yahwe kutoka mahali pake!" 13 Ilikuwa sauti ya mabawa ya viumbe
hai vilipokuwa vikigusana kila kimoja, na sauti ya magurudumu ambayo yalikuwa
pamoja na hivyo viumbe, na sauti ya tetemeko kubwa arithi. 14 Roho akaniinua juu na
kunichukua, Nikaenda kwa uchungu katika hasira kali rohoni mwangu, kwa kuwa
mkono wa Yahwe ulikuwa na nguvu ukigandamiza juu yangu! 15 Hivyo nikaenda
kwa watumwa huko Tel Abibu waliokuwa wakiishi karibu na Kebari Kanali, na
niliishi miongoni mwao huko kwa mda wa miaka saba, kushinda kabisa katika
mshangao. 16 Kisha ikatokea baada ya siku saba kwamba neno la Yahwe likanijia,
likisema, 17 "Mwana wa adamu, nimekufanya uwe mwangalizi kwa ajili ya nyumba
ya Israeli, hivyo sikiliza neno kutoka kinywani mwangu, na uwapatie onyo langu.
18 Nitakaposema kwa waovu, 'Utakufa hakika' na usimuonye au kuzungumza onyo
kwa waovu kuhusu matendo yao maovu hivyo anaweza kuishi-yule muovu atakufa
kwa ajili ya dhambi yake, lakini nitaitaka damu yake kutoka kwenye mkono wako.
19 Lakini kama ukimuonya muovo, na asiuache uovu wake au kutoka matendo yake
maovu, kisha atakufa kwa dhambi yake, lakini utaokoa maisha yako mwenyewe.
20 Kama mwenye haki ataicha haki yake na kutenda yasiyohaki, na nikaweka kizuizi
mbele yake, atakufa. Kwasababu hukumuonya, atakufa katika dhambi yake, na
sintokumbuka matendo ya haki aliyoyafanya, lakini nitaitaka damu yake kutoka
kwenye mkono wako. 21 Lakini kama ukimuonya mwenye mtu mwenye haki kuacha
kufanya dhambi halafu akaacha kutenda dhambi, ataishi hakika tangu alipo unywa;
na utakuwa umeokoa maisha yako mwenyewe." 22 Hivyo mkono wa Yahwe ulikuwa
juu yangu huko, akanambia, "Inuka! nenda uwandani, na nitaongea na wewe huko!"
23 Nikainuka na kwenda uwandani, na huko utukufu wa Yahwe ulisimama, kama
utukufu ambao niliokuwa nimeuona karibu na Kebari Kanali; hivyo nikaanguka
kifudifudi. 24 Roho akaja kwangu na kusimama juu ya miguu yangu; akaongea na
mimi, na kunambia, "Nenda na jifungie mwenyewe kwenye nyumba yako, 25 kwa
sasa, mwana wa adamu, wataweka kamba juu yako na kukufunga ili usiweze kutoka
nje miongoni mwao. 26 Nitaufanya ulimi wako ugandamane na paa ya mdomo wako,
ili kwamba uwe kimya, na hutaweza kuwakemea, kwa kuwa ni nyumba ya waasi.
27 Lakini nitakapozungumza na wewe, nitafungua mdomo wako hivyo utawaambia,
'Hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo.' Yeye asikiaye na asikie; yeye asiyesikia na
asisikie, kwa kuwa wao ni nyumba ya kuasi!"

# 4

1 "Lakini wewe, mwana wa adamu, chukua tofali wewe mwenyewe na uliweke
mbele yako. Kisha chonga mji wa Yerusalemu juu yake. 2 Kisha laza kuizunguka,
ngome juu yake. Anza kushambulia juu yake na weka makambi kuizunguka. Weka
shambulio la ghasia kuizunguka. 3 Kisha chukua kwa ajili yako mwenyewe sufuria
ya chuma na itumie kama ukuta wa chuma kati yako mwenyewe na mji na weka
uso wako dhidi yake. Kwa kuwa utazingirwa, na utaweka ukombozi juu yake. Hii
itakuwa alama kwa nyumba ya Israeli. 4 Kisha, lala juu upande wako wa kushoto
na weka dhambi ya nyumba ya Israeli juu yake; utazibeba dhambi zao kwa hesabu
za siku ambazo ulizolala juu ya nyumba ya Israeli. 5 Mimi mwenyewe nakuagiza
kwako siku moja kuwakilisha kila mwaka wa adhabu yao: siku 390! Katika njia
hii, utachukua dhambi ya nyumba ya Israeli. 6 Wakati utakapomaliza hizi siku,
kisha lala chini kwa mara ya pili kwa upande wako wa kulia, kwa kuwa utabeba
dhambi ya nyumba ya Yuda kwa siku arobaini. Nakuteua wewe siku moja kwa kila

mwaka. [7] Weka uso wako chini kuelekea Yerusalemu ambayo ni chini ya ngome,
na kwa mkono wako funua unabii dhidi [8] yake. Tazama! naweka vifungo juu yako
hivyo hutarudi kutoka upande mmoja kwenda upande mwingine hadi utakapoliza
siku zako za kuzingirwa kwako. [9] Chukua ngano kwa ajili yako, shayiri, dengu,
mtama, kusemethi; viweke kwenye chombo kimoja na tengeneza mkate kwa ajili
yako kulingana na hesabu ya siku ambazo utakazo lala katika ya upande wako. Kwa
siku 390 utaula. [10] Chakula utakachokula kitapimwa, shekeli ishirini kwa siku, na
utakila kwa mda uliopangwa kila siku. [11] Kisha utakunywa maji, kwa kuyapima
sehemu ya sita ya hini, na utayanywa kwa mda uliopangwa. [12] Utakila kama keki za
shayiri, lakini utaioka kwenye kinyesi kikavu cha mwanadamu mbele ya macho yao!"
[13] Kwa kuwa Yahwe asema, "Hii inamaana kwamba ule mkate ambao watu wa Israeli
watakula kitakuwa kinajisi, huko miongoni mwa mataifa ambapo nitakaowafukuza."
[14] Lakini nikasema, "Ee, Bwana Yahwe! Sijawahi kuwa najisi! sijawahi kula kitu
chochote ambacho kimekufa au kitu chochote kilichouawa na wanyama, kutoka
mdomoni mwangu hadi sasa, wala nyama ya kunuka haijawahi kuingia kinywani
mwangu!" [15] Ndivyo alivvyo niambia, "Tazama! Nimekupa mbolea ya ng'ombe
badala ya kinyesi cha mwanadamu ili uweze kuandaa mkate wako juu ya hayo."
[16] Pia akanambia, "Mwana wa adamu! Tazama! Nalivunja gongo la mkate katika
Yerusalemu, na watakula mkate ukiwa umepimwa katika wasiwasi na kunywa maji
kwa kuyapima katika hofu. [17] Kwa sabau watapungukiwa na mkate na maji, kila mtu
atafadhaishwa na ndugu yake na kumpoteza kwa sababu ya udhalimu wao."

# 5

[1] "Kisha wewe mwana wa adamu, chukua upanga mkali kama wembe wa kinyozi
kwa ajili yako mwenyewe, na pitisha hayo makali juu ya kichwa chako na ndevu
zako, kisha chukua mizani za kupimia uzito na uzigawanye nywele zako. [2] Choma
theluthi ya tatu ya hiyo kwa moto katikati ya mji wakati siku za kuzingirwa
zitakapokamilika, na chukua theluthi ya nywele na uipige kwa panga na kuuzunguka
mji. Kisha tawanya theluthi yake kwenye upepo, na nitasogeza panga karibu
ili kufukuza watu. [3] Lakini chukua kiasi kidogo cha nywele na zifunge kwenye
pindo za nguo yako. [4] Kisha chukua tena zile nyewele na zitupe katikati ya
moto; na zichome kwenye moto; kutoka hapo utatoka nje kwenda nyumba zote
za Israeli." [5] Bwana Yahwe asema hivi, "Hii ndio Yerusalemu katikati ya mataifa,
nilipomuweka, na ambapo nilipomzunguka kwa nchi zingine. [6] Lakini anaudhaifu
wa kukataa amri zangu zaidi kuliko mataifa yalivyo, na sheria yangu zaidi kuliko
mataifa ambayo yanayomzunguka. Watu wamezikataa humuku zangu na kuacha
kutembea katika sheria zangu." [7] Kwa hiyo Bwana Yahwe asema hivi, "Kwa sababu
mmekuwa kikwazo kuliko mataifa ambayo yanayowazunguka na kuacha kutembea
kwenye amri zangu wala kutenda kulingana na amri zangu, wala hata kutenda
kulingana na amri za mataifa yanayowazunguka," [8] kwa hiyo Bwana asema hivi,
"Tazama! Mimi mwenyewe nitatenda juu yenu. Nitato hukumu kati yenu ili
mataifa waone. [9] Nitawafanyia yale ambayo sijawahi kuyafanya na kile ambacho
sintokifanya tena, kwa sababu ya matendo yenu ya kuchukiza. [10] Kwa hiyo baba
watawala watoto kati yenu, na watoto watawala baba zao, kwa kuwa nitafanya
hukumu juu yenu na kuwatawanya kila mahali wote ninyi mliobaki. [11] Kwa hiyo,
kama niishivyo-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-bila shaka hii ilikuwa kwa
sababu umapanajisi patakatifu pangu kwa mambo ya machukizo yako yote na
kwa matendo yako yote niyachukiayo, kwamba mimi mwenyewe nitakupunguza
katika hesabu; jicho langu halitakuhurumia, na sintoacha kukuharibu. [12] Theluthi
yenu mtakufa kwa tauni, na wataliwa na njaa katikati yenu. Theluthi wataanguka

kwa upanga likiwazunguka. Kisha nitawatawanya theluthi katika mahali pote, na
nitafuatisha upanga kuwafukuza pia. 13 Hivi ndivyo ghadhabu yangu itavyokamilika,
na nitasababisha ghadhabu yangu juu yao hata kulala. Nitajiridhisha, na watajua
kwamba, mimi Yahwe, nimenena kwa ghadhabu yangu wakati nitakapo kamilisha
ghadhabu yangu dhidi yao. 14 Nitakufanya mkiwa kwa mataifa yanayokuzunguka
kwenye uso wa kila mtu apitaye karibu. 15 Hivyo Yerusalemu itakuwa jambo kwa
watu wengine kushutumu na kufanya mzaha, na chukizo kwa mataifa ambayo
yanayowazunguka. Nitafanya hukumu dhidi yenu kwa ghadhabu na hasira, na kwa
kukemea kwa hasira-Mimi, Yahwe nimesema hivi! 16 Nitatuma mishale mikali ya
njaa juu yenu ambayo itakuwa na maana ya kwamba nitawaharibu. Kwa kuwa
nitaongeza njaa juu yenu na kuvunja tegemeo lenu la mkate. 17 Nitaleta njaa na
majanga dhidi yenu hivyo mtakuwa wagumba. Tauni na damu zitapita kati yako, na
nitaleta upanga dhidi yenu-Mimi Yahwe, nimesema hivi."

# 6

1 Neno la Yahwe likanijia, likisema, 2 "Mwana wa adamu, weka uso wako dhidi
ya milima ya Israeli na uwatabirie. 3 Sema, 'Milima ya Israeli, silikilizeni neno la
Bwana Yahwe! Bwana Yahwe asema hivi kwenye milima kwenye vilele, kwenye
vijito na kwenye mabonde: Tazama! Naleta upanga dhidi yenu, na nitapaharibu
pahali penu pa juu. 4 Kisha madhabahu zenu zitakuwa ukiwa na nguzo zenu
zitaharibiwa, na nitatupa chini wafu wenu mbele ya sanamu zao. 5 Nitalaza miili
iliyokufa kwa watu wa Israeli mbele ya sanamu zao, na kuitawanya mifupa yenu
kuzizunguka madhabahu zenu. 6 Kila mahali utaishi, miji itaharibiwa na mahali
pa juu kuangamia, hivyo basi madhabahu zenu zitaharibiwa na kufanywa ukiwa.
Kisha zitavunjwa na kupotea, nguzo zenu zitaangushwa chini na kazi zenu zitafutwa
mbali. 7 Waliokufa wataanguka chini kati yenu nanyi mtajua kwamba mimi ni Yahwe.
8 Lakini nitahifadhi mabaki kwenu, na kutakuwa na wale watakao toroka upanga
miongoni mwa mataifa, 9 Kisha wale watakao toroka watanikumbuka miongoni mwa
mataifa amababo watakapochukuliwa mateka, ndivyo nitakavoyowaponda mioyo
yao ya kikahaba ambayo imeniacha, na kwa macho yao ya kikahaba kufuata sanamu
zao. Kisha wataonyesha chuki kwenye nyuso zao kwa udhaifu walioufanya kwa
machukizo yao yote. 10 Hivyo watajua kwamba mimi ni Yahwe. Kulikuwa na sababu
kwamba nimesema nitaleta huu uovu kwao. 11 Bwana Yahwe asema hivi: Piga
makofi na kanyaga kwa mguu wako! Sema! 'Ole!' kwa sababu ya uovu wote wa
chukizo wa nyumba ya Israeli! Wataanguka kwa upanga, njaa, na tauni. 12 Yule
aliye mbali sana atakufa kwa tauni, na yule aliyekaribu ataanguka kwa upanga.
Wale watakaobaki na kuishi watakufa kwa upanga. Kwa njia hii ndivyo nitakavyo
kamilisha madhabahu yangu dhidi yao. 13 Kisha mtajua kwamba mimi ni Yahwe,
wakati waliokufa watakapolala kati ya sanamu zao, kuzizunguka madhabahu, kwa
kila mlima mrefu-juu ya vilele vya mlima, na chini ya mti wenye majani mabichi na
mwalo mnene-sehemu wanapochomea ubani kwa sanamu zao zote. 14 Nitapiga kwa
mkono wangu na kuifanya nchi ukiwa na isiyofaa, kutoka jangwa hata Dibla, kupita
sehemu zote wanapoishi. Kisha watajua kwamba mimi ni Yahwe."

# 7

1 Neno la Yahwe likanijia, likisema, 2 Wewe, mwanadamu-Bwana Yahwe asema
hivi kwa nchi ya Israeli."'Mwisho! Mwisho umekuja kwenye mipaka minne ya
nchi. 3 Sasa mwisho uko juu yako, kwa kuwa natuma ghadhabu yangu juu yako,
nitakuhukumu kulingana na njia zako; nitaleta machukizo yako yote juu yako. 4 Kwa
kuwa macho yangu hayatakuhurumia, na sitakuharibu. Badala yake, nitaleta njia

zako zote juu yako, na machukizo yako yote yatakuwa katikati yako, hivyo utajua
kwamba mimi ni Yahwe. [5] Bwana Yahwe asema hivi: Msiba! Msiba wa pekee!
Tazama, unakuja. [6] Mwisho unakuja hakika. Mwisho umeamsha dhidi yenu. Tazama!
unakuja! [7] Kifo chako kinakuja kwako ukaaye kwenye nchi. Mda umefika; siku ya
uharibifu iko karibu, na milima haitakuwa na shangwe tena. [8] Sasa baada ya mda
mfupi nitamwaga dhahabu yangu juu yako na kujaza hasira yangu juu yako wakati
nitakapokuhukumu kulingana na njia zako na kuleta machukizo yako yote juu yako.
[9] Kwa kuwa jicho langu halitaona kwa huruma, sitakuharibu, kama ulivyofanya,
nitafanya kwako; na machukizo yako yatakuwa katikati yako hivyo utajua kwamba
ni mimi Yahwe, anayekuadhibu. [10] Tazama, siku! Tazama, inakuja! Kifo kimetoka!
fimbo ya kuadhibia imechanua, kiburi kimechipua! [11] Udhalimu umekua kwenye
fimbo ya udhaifu-hakuna kati yao, na hakuna katika ya kundi lao, hakuna katika
utajiri wao, na hakuna wa muhimu wao atakaye baki! [12] Muda unakuja; siku
imekaribia. Usimuache anayenunua shangwe, wala asihuzunike auzaye, kwa kuwa
hasira yangu iko juu ya kikundi kizima! [13] Kwa kuwa muuzaji hatarudia kile
kilichouzwa, kadiri wanapoendelea kuishi, kwa kuwa maono yako juu yako kikundi
kizima. Hawatarudi, kwa kuwa hakuna mtu anayeishi kwenye dhambi atakayejitia
nguvu! [14] Wamepiga tarumbeta na kufanya kila kitu tayari, lakini hakuna mtu
anayeenda kupigana; kwa kuwa hasira yangu iko juu ya kundi zima. [15] Upanga
uko nje, na tauni na njaa viko nje kwenye jengo. Wale walioko shambani watakufa
kwa upanga, wakati njaa na tauni zitakapowala wale waliopo kwenye mji. [16] Lakini
watakao salia watatoroka kutoka miongoni mwao, na watakwenda kwenye milima.
Kama hua wa mabondeni, wote watalia-kila mtu kwa ajili ya uovu wake. [17] Kila
mkono utasita na kila goti litakuwa dhaifu kama maji, na watavaa nguo za magunia,
na hofu kuu itawafunika, [18] na aibu itakuwa juu ya kila uso, na upara juu ya vichwa
vyao vyote. [19] Watatupa fedha yao kwenye mitaa na dhahabu yao itakuwa kama
jalala. Fedha yao na dhahabu yao haitaweza kuwaokoa katika siku ya ghadhabu ya
Yahwe. Maisha yao hayataokolewa, na njaa yao haitashiba, kwa sababu uovu wao
umekuwa kizuizi. [20] Kwenye fahari yao walichukua kito yake nzuri za mapambo,
pamoja nao wakatengeza sanamu zao za vinyago, na vitu vyao vichukizavyo. Kwa
hiyo, nayabadilisha haya kuwa kitu najisi kwao. [21] Kisha nitawapatia hivyo vitu
kwenye mikono ya wageni kama mateka na kwa waovu wa dunia kama mateka, na
watapanajisi. [22] Kisha nitaugeuza uso wangu mbali kutoka kwao watakapo najisi
mahali pangu pa siri; maharamia wataingia humo na kupanajisi. [23] Tengeneza
mnyororo, kwa sababu nchi imejaa hukumu ya damu, na mji umejaa udhalimu.
[24] Hivyo nitaleta waovu wengi wa mataifa, na watamilki nyumba zao, na nitaleta
mwisho kwenye fahari ya uweza, kwenda mahali pao patakatifu patanajisiwa!
[25] Hofu itakuja! Wataitafuta amani, lakini haitakuwepo. [26] Majanga juu ya majanga
yatakuja juu yangu, na kutakuwa na tetesi juu ya tetesi. Kisha watatafuta ono moja
kutoka kwa nabii, lakini sheria itawaangamiza kutoka kwa kuhani na shauri kutoka
kwa wazee. [27] Mfalme ataomboleza na mwana wa mfalme atakata tamaa, wakati
mikono ya watu wa nchi itatetemeka kwa hofu. Kulingana na njia zao wenyewe
nitafanya hivi kwao! Nitawahukumu sawa sawa na wanavyostahili hadi watakapojua
yakwamba mimi ni Yahwe.'"

# 8

[1] Hivyo ikawa kuhusu katika mwaka wa sita na mwezi wa sita, katika siku ya
tano ya mwezi, nilipokuwa nimeketi kwenye nyumba yangu na wazee wa Yuda
waliketi mbele yangu, kwamba mkono wa Bwana Yahwe ukanijaza juu yangu huko.
[2] Hivyo nikaona, na tazama, kulikuwa na mfano kama mwonekano wa mwanadamu.

Kutoka kwenye mwonekano wake wa nyonga kwenda chini kulikuwa na moto. Na
kutoka kwenye nyonga kwenda juu kulikuwa na mwonekano wa kitu kinachong'aa,
kama mng'ao wa chuma. 3 Kisha akanyoosha kutoka kwenye mkono na kunichukua
kwa nywele za kichwa changu; Roho akaniacha juu kati ya dunia na mbingu, na
katika maono kutoka kwa Mungu, akaniletea hata Yerusalemu, kwenye mlango
wa kuingia ndani ya lango la kaskazini, ambako sanamu ile iletayo wivu mkubwa
ilipokuwa imesiamama. 4 Kisha tazama, utukufu wa Mungu wa Israeli ulikuwa
huko, kulingana na ono nililokuwa nimeliona kwenye uwanda. 5 Kisha akanambia,
“Mwanadamu, inua juu macho yako kwenda upande wa kaskazini.” Hivyo nikainua
macho yangu kuelekea kaskazini, na kwenye lango la kaskazini kulekea kwenye
madhabahu, huko kwenye lango la kuingilia, kulikuwa na sanamu ya wivu. 6 Hivyo
akanambia, “Mwanadamu, unaona wanayoyafanya? Haya ni machukizo makubwa
ambayo nyumba ya Israeli wanayoyafanya hapa kunifanya niende mbali kutoka
patakatifu pangu. Lakini utageuka na kuona machukizo makubwa zaidi.” 7 Kisha
akanileta hata kwenye mlango wa uzio, na nikatazama, kulikuwa na shimo kwenye
ukuta.” 8 Akanambia, “Mwanadamu, chimba kwenye huu ukuta.” Basi nikachimba
kwenye huo ukuta, na kulikuwa na mlango. 9 Kisha akanambia, “Nenda na ukaone
machukizo ya uovu ambayo wanayoyafanya hapa.” 10 Basi nilipokuwa nikienda
ndani na nikaona, na tazama! Kulikuwa na kila umbo la vitu vikitembea polepole na
mnyama achukizaye sana! Kila sanamu wa nyumba ya Israeli ilikuwa imechongwa
kwenye ukuta pande zote. 11 Wazee sabini wa wa nyumba ya Israeli walikuwa
huko, na Yaazania mwana wa Shafani alikuwa amesimama katikati yao. Walikuwa
wamesimama mbele ya picha, na kila mtu alikuwa na chetezo kwenye mkono wake
ili kwamba harufu ya ubani ingeweza kupanda juu. 12 Akanambia, “mwanadamu,
unaona kile ambacho wazee wa nyumba ya Israeli wanachokifanya kwenye giza?
Kila mmoja hufanya hivi kwenye chumba cha sanamu yake, kwa kuwa husema,
'Yahwe hatuone! Yahwe ameitelekeza hii nchi.”' 13 Kisha akanambia, “Geuka tena
na tazama machukizo makubwa ambayo wanayoyafanya.” 14 Tena akanileta kwenye
lango la kuingia la nyumba ya Yahwe lililokuwa upande waa kaskazini, na tazama!
Wanawake walikuwa wameketi huko wakimlilia Tamuzi. 15 Hivyo akanambia,
“Umeiona hii, mwanadamu? Geuka tena na uone machukizo makubwana zaidi
kuliko hayo.” 16 Akanileta hata kwenye uzio wa ndani wa nyumba ya Yahwe, na
tazama! huko kwenye lango la kuingia kwenye madhabahu, kulikuwa na takribani
watu ishirini na tano waliokuwa wamelipa mgongo hekalu la Yahwe na nyuso
zao kuelekea mashariki, na walikuwa wakiabudu jua. 17 Akanambia, “Unaona hii,
mwanadamu? Je ni kitu kidigo kwa ajili ya nyumba ya Yuda kufanya haya machukizo
wanayoyafanya? Kwa kuwa wameijaza nchi kwa uovu na wamerudi tena ili kuniletea
hasira, kuweka tawi kwenye pua zao. 18 Hivyo nitatenda miongoni mwao pia; jicho
langu halitakuwa na huruma, sitaacha kuwaharibu. hata watalia kwenye masikio
yangu kwa sauti kubwa, sitawasikia.”

# 9

1 Kisha akalia kwa sauti kubwa nikasikia kwenye masikio yangu, huku akisema,
“Waache walinzi waje kwenye mji, kila mmoja na silaha yake ya uharibifu kwenye
mkono wake.” 2 Kisha tazama! watu wanne watakuja kutokea njia ya lango la juu
linaloelekea kaskazini, kila mmoja na silaha yake ya kuchinjia kwenye mkono wake.
Kulikuwa na mtu mmoja miongoni mwao alikuwa amevaa nguo ya kitani pamoja
na kifaa cha uandishi ubavuni mwake. Hivyo waliingia na kusimama karibu na
madhabahu ya shaba. 3 Kisha utukufu wa Mungu wa Israeli ukapanda juu kutoka
kwa kerubi ambapo ilikuwa kwenye kisingiti cha nyumba. Akamwita yule mtu

aliyekuwa amevaa nguo ya kitani na kifaa cha uandishi ubavuni mwake. 4 Yahwe
akamwambia, “Pita kati ya mji-kati ya Yerusalemu-na weka alama katika vipaji vya
uso vya wale waliolemewa na kuona kuhusu machukizo yote yanafanyika kati ya
mji.” 5 Kisha akaongea na wengine kupitia kusikia kwangu, “Pita kwenye mji baada
ya yeye na kuua. Msiache macho yenu yawe na huruma, na msiogope kuharibu 6 iwe
mzee, kijana, msichana, mtoto mdogo au wanawake. Waueni watu wote! Lakini
msimkaribie mtu yeyote ambaye mwenye alama kwenye kichwa chake. Anzeni
katika patakatifu pangu!” Hivyo wakaanza na wazee waliokuwa mbele ya nyumba.
7 Akawaambia, “Najisi nyumba, na kujaza zio zake kwa waliokufa. Endeleeni!”
Hivyo wakaenda na kuushambulia mji. 8 Walipokuwa wakiushambulia, nikajikuta
mwenyewe na nikaangukia kwenye uso wangu na kulia kwa sauti na kusema, “Ee,
Bwana Yahwe, utayaharibu mabaki yote ya Israeli wakati wa kumwaga ghadhabu
yao juu ya Yerusalemu?” 9 Akanambia, “Uovu wa nyumba ya Israeli na Yuda
unaongezeka sana. Nchi imejaa damu na mji umejaa upotovu, tangu waliposema,
'Yahwe ameisahau nchi; na Yahwe haoni!' 10 Hivyo kisha, macho yangu hataangalia
kwa huruma, na sintoacha kuwaharibu. Badala yake nitaileta juu ya vichwa vyao.”
11 Tazama! yule mtu aliyekuwa amevaa nguo ya kitani aliyekuwa na kifaa cha
uandishi kwa uapende wa ubavuni mwake. Alitoa taarifa na kusema, “Nimemaliza
yale yote uliyoniamuru.”

# 10

1 Nilipokuwa nikingalia mbele ya anga ambalo liliyokuwa juu ya vichwa vya kerubi;
kitu kikawatokea juu yao kama rangi ya samawati mwonekano wake ulikuwa kama
kiti cha enzi. 2 Kisha Yahwe akaongea na yule mtu alikuwa maevaa nguo za kitani na
kusema, “Nenda kati ya magurudumu chini ya kerubi, na jaza mikono yako yote na
watawanye juu ya mji.” Kisha yule mtu akaenda ndani nikiwa natazama. 3 Kerubi
likasimama juu ya upande wa kulia wa nyumba wakati yule mtu alipoingia, na wingu
likaja a ndani ya uzio. 4 Utukufu wa Yahwe ukainuka kutoka kwenye kerubi na
kusimama kwenye kizingiti cha nyumba. Ukaijaza nyumaba kwa wingu, na uzio
ulikuwa umejaa nuru ya utukufu wa Yahwe. 5 Sauti ya mabawa ya kerubi ikasikika
kwa mbali nje ya uzio, kama sauti ya Mungu mwenyezi wakati akiwa anaongea.
6 Ikawa kuhusu, Mungu alipoamwamuru yule mtu aliyekuwa amevaa nguo za
kitani na kusema, “Chukua moto kutoka kwenye ya kerubi,” yule mtu akaenda
na kusimama karibu na gurudumu. 7 Kerubi akaunyoosha mkono wake kwenye
kerubi kwenye moto uliokuwa miongoni mwa kerubi, na kuiacha juu na kuiweka
kwenye mikono ya yule mtu aliyekuwa amevaa vazi la kitani. Yule mtu akaichukua
na kurudi. 8 Nikaona juu ya kerubi kitu kama mkono wa mtu juu ya mabawa
yao. 9 Hivyo nikaona, na tazama! Magurudumu manne yalikuwa karibu na kerubi-
gurudumu moja karibu na kila kerubi-na mwonekano wa hayo magurudumu ulikuwa
kama jiwe la zabarajadi. 10 Mwonekano wake ulikuwa unaofanana kama wa wote
wanne, kama gurudumu lililokuwa kwenye gurudumu lingine. 11 wakati walipokuwa
wakitembea, walienda katika pande zote nne bila kugeuka katika kwenye njia
nyingine. Badala yake, popote kichwa kilipoelekea, walilifuata. Hawakugeuka
kwenye njia yeyote nyingine walipokuwa wakienda. 12 Mwili wao wote-pamoja
na migongo yao, mikono yao, na mabawa yao-vilikuwa vimefunikwa kwa macho,
na macho kufunika magurudumu manne kuzunguka pote pia. 13 Nilikuwa nasikia,
magurudumu yalikuwa yakiita, “Kuzunguka.” 14 Walikuwa na nyuso nne kila moja;
uso wa kwanza ulikuwa uso wa kerubi, uso wa pili ulikuwa uso wa mtu, uso wa
tatu ulikuwa uso wa simba, na uso wa nne ulikuwa uso wa malaika. 15 Kisha
makerubi-hawa walikuwa viumbe hai nilivyokuwa nimeviona karibu na Keberi

Kanali-wakainuka juu. [16] Popote makerubi walipoenda, magurudumu yalienda
karibu nao, na popote makerubi walipoinua juu mabawa yao kupaa juu kutoka
kwenye nchi, magurudumu hayakugeuka. Yaliendelea kuwa karibu nao. [17] Wakati
makerubi waliposimama, magurudumu yalisimama pia, na wakati walipoinuka
juu, magurudumu yaliinuka juu pamoja nao, kwa kuwa roho wa vile viumbe hai
walikuwa kwenye magurudumu. [18] Kisha utukufu wa Yahwe ukaja kutoka juu ya
kizingiti cha nyumba na kusimama juu ya kerubi. [19] Lile kerubi likaacha juu mabawa
na kuinuka kutoka kwenye jicho langu wakati walipotoka nje, na yale magurudumu
yakafanya vivyo hivyo karibu yao. Wakasimama upande wa mashariki kuingia
kwenye nyumba ya Yahwe, na utukufu wa Mungu wa Israeili ukaja juu yao kutoka
juu. [20] Hawa walikuwa viumbe hai ambao niliokuwa nimewaona chini ya Mungu
wa Israeli karibu na Kebari Kanali, hivyo nilijua kwamba walikuwa makerubi!
[21] Walikuwa na macho manne kila mmoja na mabawa manne, na mfanano wa nyuso
zao zilikuwa na mfanano wa mikono ya mwanadamu chini ya mabawa yao, [22] na
mfanano wa nyuso zao ulikuwa kama nyuso nilizokuwa nimeziona kwa maono huko
Keberi Kanali, na kila mmoja wao alienda mbele.

# 11

[1] Kisha Roho akaniacha juu na kunileta kwenye lango la mashariki la nyumba ya
Yahwe, kuelekea mashariki, na tazama, kwenye njia ya mlango wa lango kulikuwa
na watu ishirini na tano. Nikamwona Yaazania mwana wa Azuri na Pelatia mwana
wa Benaya, viongozi wa watu, miongoni mwao. [2] Mungu akanambia, “Mwana wa
adamu, hawa ndio wale watu walioshauri udhalimu, na kuamua mipango miovu
kwenye huu mji. [3] Wakisema, 'Mda wa kujenga nyumba sio sasa; huu mji ni sufuria,
na sisi ni nyama.' [4] Kwa hiyo tabiri juu yao. Tabiri, mwana wa adamu.”' [5] Kisha Roho
wa Yahwe akanijaza na akaniambia, “akisema: Hivi ndivyo Yahwe asemavyo: kama
usemavyo, nyumba ya Israeli; kwa kuwa najua kinachoendelea kwenye fikra zenu.
[6] Mmewazidisha watu mliowaua kwenye huu mji na kuijaza mitaa kwa hao. [7] Kwa
hiyo, Bwana Yahwe asema hivi: Wale watu milowaua, ambao mmeilaza miili yao
kati ya Yerusalemu, ni nyama, na huu mji ni sufuria. Lakini mnaenda kutolewa nje
kutoka kati ya huu mji. [8] Mmeuogopa upanga, kwa hiyo nauleta huo upanga juu yenu-
huu ndio usemi wa Bwana Yahwe. [9] Nitawatoa nje kutoka kati ya mji, na kuwaweka
kwenye mikono ya wageni, kwa kuwa nitaleta hukumu dhidi yenu. [10] Mtaanguka kwa
upanga. Nitawahukumu kati ya mipaka ya Israeli hivyo mtajua yakwamba mimi ni
Yahwe. [11] Huu mji hautakua sufuria yenu ya kupikia, wala hamtakuwa nyama ndani
yake. Nitawahukumu kati ya mipaka ya Israeli. [12] Kisha mtajua yakwamba mimi ni
Yahwe, yule ambaye hamuishe kwenye amri zake na ambaye hamkuzishika sheria
zake. Badala yake, mmebeba hukumu za mataifa wanayowazunguka.” [13] Ikawa
kwamba nilipokuwa natabiri, Pelatia mwana wa Benaya, akafa. Hivyo nikaanguka
kwenye uso wangu na kulia kwa sauti na kusema, “Ee, Bwana Yahwe, Je utayaharibu
kabisa mabaki ya Israeli?” [14] Neno la Yahwe likanijia, likisema, [15] “Mwana wa
adamu, ndugu zako! Ndugu zako! Watu wa ukoo wako na nyumba yote ya Israeli!
Wote hao ndio hao ambao inasemekana wale wanaoishi Yerusalemu, 'Wako mbali
sana kutoka kwa Yahwe! Hii nchi tulipewa sisi kama milki yetu.' [16] Kwa hiyo
sema, 'Bwana Yahwe asema hivi: kote nimewapitisha mbali kati ya mataifa, na
kote nimewasambaza kati ya nchi, bado nimekuwa patakatifu kwa ajili yao kwa
mda kidogo kwenye nchi ambazo walizoenda.' [17] Kwa hiyo sema, 'Bwana Yahwe
asema hivi: Nitawakusanya kutoka kwa watu, na kuwakutanisha kutoka kwenye
nchi mlizokuwa mmetawanyika, na nitawapatia nchi ya Israeli.' [18] Kisha wataenda
huko na kuondoa kila kitu chenye karaha na kila chukizo kutoka hiyo sehemu.

[19] Nitawapatia moyo mmoja, na nitaweka roho mpya kati yao. Nitaondoa moyo wa
jiwe kutoka kwenye miili wao na kuwapatia moyo wa nyama, [20] ili kwamba waweze
kutembea kwenye amri zangu, watayachukua maagizo yangu na kuyatenda. Kisha
watakuwa watu wangu, na nitakuwa Mungu wao. [21] Lakini kwa wale watembeao
kwa kujifanya kuendeleza mambo yao ya karaha na machukizo yao, nitaleta tabia yao
kwenye vichwa vyao-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo." [22] Makerubi wakainua
mabawa yao na magurudumu yaliyokuwa karibu nao, na utukufu wa Mungu wa
Israeli ulikuwa juu yao. [23] Kisha utukufu wa Yahwe ukaenda juu kutoka katikati
ya mji na kusimama kwenye mlima hata mashariki mwa mji. [24] Roho akanichukua
juu na kunileta hata Ukaldayo, hata uhamishoni, katika maono kutoka kwa Roho
wa Mungu, na maono niliyokuwa nimeyaona yakaenda juu yakaniacha. [25] Kisha
nikawaambia wale watumwa mambo yote ya Yahwe niliyokuwa nimeyaona.

# 12

[1] Neno la Yahwe likanijia, kusema, [2] "Mwana wa adamu, unaishi kwenye nyumba
ya uasi, wana macho ya kuona lakini hawaoni; na wana masikio ya kusikia lakini
hawasikii, kwa sababu wao ni nyumba iliyoasi. [3] Kwa hiyo wewe mwanadamu, andaa
mambo yako kwa ajili ya uhamisho, na anza kuondoka mchana usoni kwao, kwa
kuwa nitakuhamisha kwenye uso wao kutoka sehemu yao kwenda sehemu nyingine.
Labda wataanza kuona, kuwa wao ni nyumba ya uasi. [4] Utatoa vitu vyako kwa ajili ya
kuhamisha mchana katika macho yao; toka jioni kwenye macho yao kama ambavyo
uendavyo kwenye uhamisho. [5] Chimba shimo ukutani kwenye uso wa macho yao,
na ingia ndani yake. [6] Kwenye macho yao, chukua vitu vyako kwenye mabega yako,
na uwalete kwenye giza. Funika uso wako kama ishara kwenye nyumba ya Israeli."
[7] Hivyo nikafanya hivyo, kama nilivyokuwa nimeamriwa. Nikatoa vitu vya uhamisho
wakati wa mchana, na katika jioni nikachimba shimo hata kwenye ukuta kwa mkono.
Nikachukua vitu vyangu kwenye giza, na kuviweka juu kwenye bega langu katika
macho yao. [8] Kisha neno la Yahwe likanijia asubuhi, likisema, [9] Mwanadamu,
je nyumba ya Israeli, ile ni nyumba ya uasi, hawakukwambia, 'Unafanya nini?'
[10] Waambie, 'Bwana Yahwe asema hivi: hili tendo la kinabii linamhuusu mwana
wa mfalme wa Yerusalemu, na nyumba yote ya Israeli walio kati yao.' [11] Sema, 'Mimi
ni ishara kwenu. Kama nilivyofanya, itafanyika kwao; watakwenda uhamishoni
na kuwa wafungwa. [12] Yule mwana wa mfalme aliye miongoni mwao atavibeba
vitu vyake kwenye bega lake katika giza, na ataenda zake kupitia kwenye ukuta.
Watachimba kwenye ukuta na kutoa vitu vyao nje. Atafunika uso wake, hivyo
hataona nchi kwa macho yake. [13] Nitausambaza wavu wangu juu yake naye atanaswa
kwenye mtego wangu; kisha nitamleta Babeli, ncha ya Wakaldayo, lakini hataiona.
Atafia huko. [14] Pia nitatawatawanya katika kila mwelekeo wale wote waliomzunguka
wanaomsaidia na jeshi lake lote, na nitaufuata upanga nyuma yao. [15] Kisha watajua
kwamba mimi ni Yahwe, wakati nitakapo watawanya kwenye nchi zote. [16] Lakini
nitaacha kuwaangamiza watu wachache kutoka miongoni mwao kutoka kwenye
upanga, njaa, na tauni, hivyo wanaweza kukumbuka maovu yao yote katika nchi
zao nilipowachukulia, hivyo watajua kwamba mimi ni Yahwe."' [17] Neno la Yahwe
likanijia, likisema, [18] "Mwanadamu, kula mkate wako kwa kutetemeka, na kunywa
maji yako kwa mtetemo na hofu. [19] Kisha waambie watu wa nchi, 'Bwana Yahwe
asema hivi kuhusiana na wale wakaao Yerusalemu, na nchi ya Israeli: Watakula
mikate yao kwa kutetemeka na kunywa maji yao wakiwa wanatetemeka, kwa kuwa
nchi itaporwa vitu vyote viijazavyo kwa sababu ya kuwa kinyume na waishio
huko. [20] Hivyo ile miji iliyokuwa wenyeji itachukuliwa, na nchi itakuwa ukiwa;
hivyo mtajua kwamba mimi ni Yahwe."' [21] Tena neno la Yahwe likanijia, likisema,

[22] “Mwanadamu, je ni mithali gani hii mlio nayo katika nchi ya Israeli mliyoisema,
'Siku zimerefushwa, na kila ono linaanguka'? [23] Kwa hiyo, waambie, 'Bwana Yahwe
asema hivi: Nitaweka mwisho wa hii mithali, na watu wa Israeli hawataitumia tena.'
Waambie, 'Siku zi karibu wakati kila ono litatimizwa. [24] Kwa kuwa hakutakuwa na
maono ya uongo yoyote wala upendeleo wa mgawanyiko kati ya nyumba ya Israeli.
[25] Kwa kuwa mimi Yahwe! Nimesema, na nitayatiza yale maneno nilyoyasema.
Hakuna kitu kitakacho chelewesha. Kwa kuwa nitaongea hili neno katika siku zenu,
nyumba ya uasi, na nitalitimiza! -hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo.”” [26] Tena
neno la Yahwe likanijia, likisema, [27] “Mwanadamu! Tazama, nyumba ya Israeli
imesema, 'Lile ono alionalo ni kwa siku nyingi kutoka sasa, na ametabiri kipindi
kilicho mbali sana.' [28] Kwa hiyo waambie, 'Bwana Yahwe asema hivi: Neno langu
halitacheleweshwa sana, lakini lile neno nililoliongea litatimizwa-hivi ndivyo Yahwe
asemavyo.'”

# 13

[1] Tena, neno la Yahwe likanijia, kusema, [2] “Mwanadamu, tabiri dhidi ya manabii
wanaotabiri katika Israeli, na uwaambie wale wanotabiri nje ya fikra zao wenyewe,
'Lisikilizeni neno la Yahwe. [3] Bwana Yahwe asema hivi: Ole wao manbii wajinga
ambao wafwatao roho zao wenyewe, lakini wale wasioona kitu! [4] Israeli, manabii
zako wamekuwa kama mbeha kwenye aridhi iliyoharibiwa na vita. [5] Hamkwenda
kwenye nyufa katika ukuta uliozunguka nyumba ya Israeli kwa ajili ya kuukarabati,
ili kupigana katika vita katika siku ya Yahwe. [6] Watu wameona uongo na kufanya
utabiri wa uongo, wale wasemao, “Hivi na hivi ndvyo Yahwe asemavyo.” Yahwe
hajawatuma, lakini hata hivyo wamewafanya watu kutumaini kwamba ujumbe wao
utakuwa kweli. [7] Je hamkusikia maono ya uongo na kufanya utabiri wa uongo,
ninyi msemao, “Hivi na hivi ndivyo Yahwe asemavyo” Wakati mimi mwenyewe
sikuongea?' [8] Kwa hiyo Bwana Yahwe asema hivi, 'Kwa sababu mmesikia maono
ya uongo na kuwaambia uongo-kwa hiyo hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo dhidi
yenu: [9] Mkono wangu utakuwa juu yenu ninyi manabii mliodanganya maono na
wale waliofanya unabii wa uongo. Hawatakuwepo kwenye kusanyiko la watu
wangu, au kuandikishwa katika kumbukumbu ya nyumba ya Israeli; hawataenda
kwenye nchi ya Israeli. Kwa kuwa mtajua yakwamba mimi ni Bwana Yahwe!
[10] Kwa sababu hiyo, na kwa sababu wamewaongoza watu wangu kuwapotosha
na kusema, “Amani!” wakati hakuna amani, wanajenga ukuta ambao wataupaka
rangi ya chokaa.' [11] Waambie wale wanaopaka chokaa ukuta, 'Utaanguka chini;
kutakuwa na mvua ya kufurika, na nitaleta mvua ya mawe kuufanya uanguke
chini, na upepo wa dhoruba kupuliza hata kuuvunja chini. [12] Tazama, ukuta
utaanguka chini. Je wengine hawakuwaambia, “Iko wapi chokaa mliyoipaka juu
yake?” [13] Kwa hiyo Bwana Yahwe asema hivi: Nitaleta upepo wa dhoruba katika
ghadhabu yangu, na kutakuwa na mafuriko ya mvua kwenye ghadhabu yangu!
Mvua ya mawe katika ghadhabu yangu itauharibu kabisa. [14] Kwa kuwa nitaurarua
chini ukuta ambao mlioufunika kwa chokaa, na nitaubomoa hata kwenye nchi na
kuifunua misingi yake. Hivyo utaanguka, nanyi nyote mtaangamizwa katikati ya
huo. [15] Ndivyo nitakavouangamiza kwa ghadhabu yangu ukuta na wale walioupaka
chokaa. Nitawaambia, “Ukuta hautaonekana tena, wala watu wanaoupaka chokaa-
[16] manabii wa Israeli wale waliotabiri kuhusu Yerusalemu na wale waliokuwa
wameona amani kwa ajili yake. Lakini hakuna amani! -hivi ndivyo Bwana Yahwe
asemavyo.” [17] Hivyo wewe, mwanadamu, weka uso wako dhidi ya binti za watu
wako wale wanaotabiri kwa akili zao wenyewe, na kutabiri dhidi yao. [18] Sema,
'Bwana Yahwe asema hivi: Ole kwa wanawake washonao hiziri kwenye kila sehemu

ya mkono wao na kutengeza vitambaa vya shela kwa ajili ya vichwa vyao kwa
kila kipimo, ili kuwinda watu. Je mtawawinda watu wangu ila kuokoa maisha
yenu wenyewe? 19 Ninyi mmenikufuru mbele ya watu wangu kwa ajili ya makonzi
ya shayiri na vipande vya mkate, kuwaua watu ambao hawakutakiwa kufa, na
kuyalinda maisha ya wale ambao hawatakiwi kuendelea kuishi, kwa sababu ya uongo
wenu kwa watu wangu walio wasikiliza. 20 Kwa hiyo Bwana Yahwe asema hivi: Niko
kinyume dhidi ya hirizi ambazo mlizozitumia kuyakamata kwa hila maisha ya watu
kana kwamba wamekuwa ndege. Naam, nitazichana kutoka kwenye mikono yenu;
na wale watu mlio wadega kama ndege-nitawaacha waende huru. 21 Nitavichana
mbali vitambaa vya shela na kuwaokoa watu wangu kutoka kwenye mikono yangu,
kwa hiyo hawatategwa tena kwenye mikono yenu. Mtajua kwamba mimi ni Yahwe.
22 Kwa sababu mmeuvunja moyo wa mtu mwenye haki kwa uongo, ingawa hata
mimi sikutamani kuvunjwa kwake moyo, na kwa sababu mmemtia moyo badala
yake matendo ya mtu mwovu ili kwamba asitaweze kurudi kutoka kwenye njia yake
kuokoa maisha yake- 23 kwa hiyo hamtayaona tena maono ya uongo au kuendelea
kufanya utabiri, kwa kuwa nitawaokoa watu wangu kutoka kwenye mkono wako.
Nanyi mtajua kwamba mimi ni Yahwe.'"

# 14

1 Baadhi ya viongozi wa Israeli wakaja kwangu na kuketi mbele yangu. 2 Ndipo
neno la Yahwe likanijia, likisema, 3 "Mwanadamu, hawa watu wamchukua sanamu
zao kwenye mioyo yao na kuweka pingamizi la uovu wao mbele ya nyuso zao
wenyewe. Je naweza kuulizwa yote na wao? 4 Kwa hiyo watangazie hivi na waambie,
'Bwana Yahwe asema hivi: Kila mtu wa nyumba ya Israeli achukuaye sanamu
moyoni mwake, au awekeye pingamizi la uovu mbele ya uso wake, na kisha yule
ajaye kwa nabii-Mimi, Yahwe, nitamjibu kulingana na sanamu zake. 5 Nitafanya
hivi ili kwamba niweze kuirudisha nyumba ya Israeli katika mioyo yao ambayo
ilikuwa mbali nami kwa ajili ya sanamu zao.' 6 Kwa hiyo sema kwa nyumba
ya Israeli, 'Bwana Yahwe asema hivi: Tubuni na rudini kutoka kwenye sanamu
zenu! Rudisheni nyuma nyuso zenu kutoka kwenye kachukizo yenu yote. 7 Kwa
kuwa kila mmoja kutoka kwenye nyumba ya Israeli na kila mmoja wa wageni
wanaoishi katika Israeli ajitengaye nami, achukuaye sanamu zake kwenye moyo
wake na kuweka kwazo la uovu wake mbele ya uso wake mwenyewe, na kisha
yule ajaye kwa nabii kunitafuta-mimi, Yahwe, nitamjibu mimi mwenyewe. 8 Hivyo
nitauweka uso wangu juu ya huyo mtu na kumfanya ishara na mithali, kwa kuwa
nitamkata kutoka kati ya watu wangu, na mtajua kuwa mimi ni Yahwe. 9 Kama
nabii atadanganywa na kuongea ujumbe, kisha Mimi Yahwe, nitamdanganya huyo
nabii; Nitanyoosha mkono wangu na kumwangamizaku toka kati watu wangu Israeli.
10 Watabeba uovu wao wenyewe; uwovu wa nabii utakua uleule kama uovu wa
yule aulizaye kutoka kwake. 11 Kwa sababu hiyo basi, nyumba ya Israeli haitaenda
mbali kutoka kunifuata mimi wala kujinajisi wenyewe kupitia dhambi zao zote.
Watakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wao-hivi ndivyo Yahwe asemavyo."'
12 Kisha neno la Yahwe likanijia, likisema, 13 "Mwanadamu, wakati nchi itakapo asi
dhidi yangu kwa kufanya dhambi ili kwamba ninyooshe mkono wangu dhidi yake
na kuvunja tegemea la mkate wake, na kuleta njaa juu yake na kukata mnyama
kutoka kwenye nchi; 14 kisha hata kama hawa watu watatu-Nuhu, Danieli, na Ayubu-
walikuwa katikati ya nchi, wangeweza kuokoa maisha yao wenyewe kwa haki-hivi
ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. 15 Kama nikileta wanyama waovu kwenye nchi
na kuwafanya wasizae hivyo basi itakuwa hakuna mtu asiweze kupita kwa sababu
ya hao wanyama, 16 kisha hata kama watu hawa hawa watatu ndani yake-kama

niishivyo, asema Bwana Yahwe-wasingeweza kuwaokoa hata watoto wao wala binti;
isipokuwa maisha yao yataokoka, lakini nchi itakuwa ukiwa. 17 Au nikileta upanga
juu ya hiyo nchi na kusema, 'Upanga, nenda kwenye nchi na wakate wote mtu na
mnyama kutoka huo', 18 kisha hata kama hawa watu watatu watakuwa katikatai
ya nchi-kama niishivyo, asema Bwana Yahwe-wasingeweza kuwaokoa japo watoto
wao wala binti; ila tu maisha yao wenyewe yangeokolewa. 19 Au kama nikipeleka
tauni juu ya nchi na kumwaga dhahabu yangu juu yake kwa damu, ili kuwakata
mtu na mnyama, 20 kisha hata kama Nuhu, Danieli, na Ayubu wangekuwa kwenye
hiyo nchi-kama niishivyo, asema Bwana Yahwe-wasingeweza kuokoa hata watoto
wao au binti; maisha yao pekee yangeokoka kwa haki. 21 Kwa kuwa Bwana Yahwe
asema hivi: hakika nitafanya mambo makali sana kwa kuleta adhabu zangu nne-
njaa, upanga, wanyama wa porini, na tauni-juu ya Yerusalemu kuwakata wote mtu
na mnyama kutoka kwake. 22 Kisha, tazama! mabaki yatasalia kwake, watakaokoka
wataenda pamoja na wana na binti. Tazama! Watawatokea, na mtaona njia zao
na matendo yao yakiwafariji kuhusu adhabu niliyoipeleka Yerusalemu, na kuhusu
kila kitu kingine ambacho nilichopeleka juu ya nchi. 23 Waliokoka watawafariji ninyi
mtakapoona njia zao na matendo yao, hivyo mtayajua haya mambo niliyoyafanya
juu yake, kwamba sijayafanya bure! -hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo."

# 15

1 Kisha neno la Yahwe likanijia, liksema, 2 "Mwanadamu, je ni jisni gani mzabibu
ulivo bora kuliko mti na matawi yaliyomo kwenye miti katika msitu? 3 Je watu
huwa wanachukua mbao kutoka kwenye mzabbibu kufanyia chochote? au huwa
wanatengenezea vitu kutokana na huo kuning'iniza chochote juu ya huo? 4 Tazama!
Kama umetupwa kwenye moto kama kuni, na kama moto umezichoma ncha zake
zote na katikati pia, je unafaa kwa chochote? 5 Tazama! Wakati ulipokuwa
umekamilika, haukuweza kufanya chochote; kisha hakika, wakati moto ulipouchoma,
lakini bado haukuweza kutengeneza kitu chochote kwa ajili ya matumizi yoyote.
6 Kwa hiyo Bwana Yahwe asema hivi: haufanani na miti katika misitu, niliyoitoa
mzabibu kama kuni kwa moto; nitatenda vivyo hivyo mbele ya wakaao Yerusalemu.
7 Kwa kuwa nitauweka uso wangu juu yao. Ingawa watatoka kutoka kwenye moto,
bado moto utawala; hivyo mtajua kwamba mimi ni Yahwe, wakati nitakapoona
uso wangu juu yenu. 8 Kisha nitaifanya nchi kuwa ukiwa kwa sababu wamefanya
dhambi-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo."

# 16

1 Kisha neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 "Mwanadamu, mwambie Yerusalemu
kuhusu machukizo yake, 3 na useme, 'Bwana Yahwe asema hivi kwa Yerusalemu:
Mwanzo wako na kuzaliwa kwako kulichukua nafasi katika nchi ya Kanaani; baba
yako alikuwa Mwamori, na mama yako alikuwa Mhiti. 4 Katika siku ya kuzaliwa
kwako, mama yako hakukata kitovu chako, wala hakukuosha kwenye maji usafishwe
au kukuchua kwa chumvi, wala kukusitiri nguo. 5 Hakuna jicho lililokuhurumia
kufanya haya mambo kwa ajili yako, kukuhurumia wewe. Katika siku uliyozaliwa,
kwa kuchukiwa uhai wako, ulitupwa nje uwandani. 6 Lakini nilipita karibu nawe,
nalikuona ukijinyonga kwa damu yako mwenyewe, "kubaki hai!" 7 Nimekufanya
ukue kama mmea katika shamba. Umeongezeka na kuwa mkubwa, na umekuwa
mzuri wa wazuri. Maziwa yako yakawa thabiti, na nywele zako zikawa nyingi,
ingawa ulikuwa uchi huna nguo. 8 Nilipita karibu nawe tena, na nalikuona.
Tazama! wakati wa upendo umefika kwako, hivyo nikatandika joho langu juu

yako na kufunika uchi wako. Kisha nikaapa kwako na kukuleta kwenye agano-
hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-na ukawa wangu. 9 Basi nilikuosha kwa maji
na kukufuta damu yako, na kukupaka mafuta. 10 Nilikuvalisha nguo ya taraza na
kukuwekea makuzi ya ngozi kwenye miguu yako. Nilikufungia kwa kitani kizuri
na kukufunika kwa hariri. 11 Kisha nalikupamba kwa vito, na kukuvalisha vikuku
kwenye mikono yako, na mkufu kwenye shingo yako. 12 Nalitia hazama katika pua
yako na hereni katika masikio yako, na taji nzuri juu ya kichwa chako. 13 Hivyo
ulipambwa kwa dhahabu na fedha, na ulivaa kitani safi, hariri, na ngu za taraza;
ulikula unga mzuri, asali, na mafuta, na ulikuwa mzuri sana, na ukawa malkia.
14 Umaarufu wako ukaenda miongoni mwa mataifa kwa sababu ya uzuri wako, kwa
kuwa ulikuwa mkamili katika ukuu niliokuwa nimekupa-hivi ndivyo Bwana Yahwe
asemavyo. 15 Lakini ulitumaini uzuri wako, na ukafanya kama kahaba kwa sababu ya
umaarufu wako; umeyamwaga matendo yako ya kikahaba kwa kila aliyepita karibu,
ili kwamba uzuri wako uwe wake. 16 Kisha ulichukua nguo zako na pamoja nao
umepatengeneza mahali pa juu kwa ajili yako palipambwa kwa rangi tofauti tofauti,
na hapo ulifanya kama kahaba. Hii haitatokea. Wala haitatokea. 17 Umevichukua
vito vizuri vya dhahabu na fedha nilizowapatia, na umejitengenezea sanamu za
wanaume, na umefanya pamoja nao ukahaba afanyao. 18 Ulichukua nguo zako za
tarizi na kuwafunika, na kuwawekea mafuta yangu na manukato mbele yao. 19 Mkate
wangu niliokupatia-ulitengenezwa kwa unga mzuri, mafuta, na asali-umeviweka
mbele yao kwa ajili ya kunukia harufu nzuri, kwa kuwa hivi ndivyo ilivyotokea-hivi
ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. 20 Kisha uliwachukua watoto wako ulionizalia, na
kuwatoa sadaka kwa picha ili waliwe kama chakula. Je! matendo yako ya kikahaba
ni kitu kidogo? 21 Umewachinja watoto wangu na kuwatupia kwenye moto. 22 Katika
machukizo yako yote na matendo yako ya kikahaba hukutafakari kuhusu siku za
ujana wako, wakati ulipokuwa uchi na bila nguo kama kama umepigwa katika damu.
23 Ole! Ole wako! -hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-kwahiyo, zaidi ya hapo kwa
haya maovu yote, 24 umejijengea chumba cha chini kwa chini katika kila sehemu
ya watu wengi. 25 Umepajenga mahali pako palipoinuka kwenye kichwa cha kila
njia na kuunajisi uzuri wako, kwa kuwa umeutoa mwili wako kwa kila mtu apitaye
karibu na umefanya matendo mengi zaidi ya ukahaba. 26 Umetenda kama kahaba
pamoja na Wamisri, tamaa ya jirani zako, na umetenda matendo mengi zaidi ya
kikahaba, ili kuchochea hasira yangu. 27 Tazama! Nitakunyooshea mkono wangu
na kupunguza chakula chako. Nitauchukua uhai wako juu ya adui zako, binti za
Wafilisti, ambao walikuwa na haya ya tabia yako ya uchafu. 28 Umetenda kama
kahaba pamoja na Waashuru kwa sababu hukuweza kuridhika. Umetenda kama
kahaba na bado hukuridhika. 29 Umefanya matendo mengi zaidi ya kikahaba katika
nchi ya jamii ya wana maji wa Ukaldayo, na wala hukuridhika kwa hayo. 30 Jinsi
moyo wako ulivyo dhaifu-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-kwamba utaweza
kuyafanya haya mambo yote, matendo ya aibu ya kikahaba? 31 Mmepajenga mahali
penu pa juu kwenye kichwa cha kila mtaa na kufanya chumba cha chini kwa chini
katika kila sehemu ya watu wengi. Bado hukuwa kama kahaba kwa sababu ulikataa
kulipwa ujira. 32 Wewe mwanamke mzinifu, wewe upokeaye wageni badala ya
mume wako. 33 Watu hulipa kwa kila kahaba, lakini wewe huwapa mshara wako
wapenzi wako wote na kuwapa rushwa ili waje kwako pande zote kwa matendo
yako ya kikahaba. 34 Hivyo kuna tofauti kati yako na hao wanawake wengine,
kwa kuwa hakuna hata mmoja ajaye kwako kukuuliza kulala pamoja nao. Badala
yake, unawalipa. Hakuna akulipaye. 35 Kwa hiyo, wewe kahaba, lisikilize neno
la Yahwe. 36 Bwana Yahwe asema hivi: Kwa sababu umemwaga tamaa yako na
kuonyesha sehemu zako za siri kupitia matendo yako ya ukahaba pamoja na wapenzi

wako wote pamoja na sanamu zako za chukizo, na kwa sababu ya damu ya watoto
wako uliyowapatia sanamu zako, 37 kwa hiyo, tazama! Nitawakusanya wapenzi
wako wote uliokutana nao, wote ambao uliowapenda na wote uliowachukia, na
nitawakusanya juu yako kila upande. Nitawaonyesha wazi sehemu zako za siri
hivyo wanaweza kuona uchi wako wote. 38 Kwa kuwa nitakuadhibu kwa uasherati
na kumwaga damu, na nitaleta juu yako damu ya hasira yangu na hasira kali.
39 Nitakutia kwenye mikono yao hivyo watakutupa chini kwenye chumba cha chini
kwa chini na kupavunja mahali pako pa juu na watakuvua nguo zako na kuchukua
vito vyako vyote. watakuacha uchi bila nguo. 40 Kisha wataleta kundi la watu juu
yako na kukupiga kwa mawe, na kukukata kwa panga zao. 41 Watachoma nyumba
zako na kufanya matendo mengi ya adhabu juu yako kwenye uso wa wanawake
wengi, kwa kuwa nitakusimamisha ukahaba wako, na hutawalipa tena wapenzi
wako. 42 Kisha nitatuliza ghadhabu yangu juu yako; hasira yangu itakuacha, kwa
kuwa nitaridhika, na sitakuwa na hasira tena. 43 Kwa sababu hukuzikumbuka siku
za ujana wako na kunifanya nitetemeke kwa hasira kwa sababu ya haya mambo
yote, kwa hiyo, tazama! Mimi mwenyewe nitashusha kwa kichwa chako mwenyewe
adhabu kwa kile ulichokifanya-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. Hutaongeza
ukahaba kwa matendo yako yote ya machukizo? 44 Tazama! Kila mtu azungumzaye
Mithali kuhusu wewe atasema, "Kama alivyo, hivyo pia ni binti yake." 45 Wewe ni
binti wa mama yako, amchukiaye mume wake na mtoto wake, na wewe ni dada
wa dada zako aliyewachukia waume zao na watoto wao. Mama yako alikuwa
Mhiti, na baba yako alikuwa Mwamori. 46 Dada yako mkubwa alikuwa Samaria na
binti zake walikuwa wale waliokuwa wakiishi kaskazini, wakati dada yako mdogo
alikuwa ni yule aliyekuwa akiishi kusini mwako, ambaye ni, Sodoma na binti zake.
47 Hukuenenda katika njia zao na kuchukua tabia zao na matendo yao, lakini katika
njia zako zote ulikuwa mbaya zaidi kuliko walivyokuwa wao. 48 Kama niishivyo- hivi
ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-dada yako Sodoma na binti zake, hawajafanya uovu
mwingi kama wewe ulivyofanya na binti zako walivyofanya. 49 Tazama! Hii ilikuwa
dhambi ya dada yako Sodoma: Alikuwa na kiburi katika mafanikio yake, uzembe
na kutojali kuhusu chochote. Hakuitia nguvu mikono ya maskini na watu wahitaji.
50 Alikuwa na kiburi na kufanya machukizo mbele yangu, hivyo niliwatoa kama
nilivyoona. 51 Samaria hakufanya hata nusu ya dhambi zako; badala yake, umefanya
machukizo mengi kuliko walivyofanya, na umewonyesha hayo dada zako walikuwa
bora kuliko wewe kwa sababu ya machukizo yako uyafanyayo! 52 Hasa wewe,
umeonyesha aibu yako mwenyewe; kwa njia hii umewaonyesha dada zako walikuwa
bora kuliko wewe, kwa sababu ya dhambi ulizozifanya katika hayo machukizo yako
yote. Dada zako sasa wanaonekana bora kuliko wewe. Hasa wewe, umeonyesha aibu
yako mwenyewe, kwa njia hii umewaonyesha kwamba dada zako walikuwa bora
kuliko wewe. 53 Kwa kuwa nitarudisha masalia wao-masalia ya Sodoma na binti zake,
na masalia ya Samaria na binti zake; lakini masalia yako yatakuwa miongoni mwao.
54 Kwa kufikiria haya mambo utaonyesha aibu yako; utakuwa mnyenyekevu kwa
sababu ya kila kitu ulichokifanya, na kwa njia hii utakuwa faraja kwao. 55 Hivyo dada
yako Sodoma na binti zake watarudishwa kwenye hali yao ya zamani, na Samaria
na binti zake watarudishwa kwenye mashamba yao ya zamani. Kisha wewe na binti
zako watarudishwa kwenye hali yako ya kawaida. 56 Sodoma dada yako hakutajwa
hata kwa kinywa chako katika siku ulipojiinua, 57 kabla uovu wako haujafunuliwa.
Lakini sasa wewe ni kitu cha dharau kwa binti za Edomu na binti wote wa Wafilisti
waliomzunguka. Watu wote wanakudharau wewe. 58 Utaonyesha aibu yako na
matendo yako ya machukizo! -hivi ndivyo Yahwe asemavyo! 59 Bwana Yahwe
asema hivi: Nitashughulika na wewe kama unavyostahili, wewe uliyedharau kiapo

chako kwa kulivunja agano. 60 Lakini mimi mwenyewe nitalikumbuka agano langu
nililolifanya pamoja nawe katika siku za ujana wako, nitaliimarisha agano la milele
pamoja na wewe. 61 Kisha utazikumbuka njia zako na kuona aibu utakapo wapokea
dada zako wakubwa na dada zako wadogo. Nitakupatia wao kama binti zako, lakini
kwa sababu ya agano lako. 62 Mimi nitaweka imara agano lango pamoja nawe, nawe
utajua yakwamba mimi ni Yahwe. 63 Kwa sababu ya haya mambo, utakumbuka
kila kitu na kuona aibu, hutafungua mdomo wako tena kuongea kwa sababu ya
aibu yako, wakati nitakapokusamehe kwa yale yote uliyoyafanya-hivi ndivyo Bwana
Yahwe asemavyo."'

# 17

1 Neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 "Mwanadamu, tega kitendawili na sema
fumbo kwa nyumba ya Israeli. 3 Sema, 'Bwana Yahwe asema hivi: Tai mkubwa
pamoja na mabawa makubwa na vipapatio virefu, mwenye kujaa manyoya, na
aliyekuwa na rangi nyingi alienda Lebanoni na kuchukua kilele cha mti wa mkangazi.
4 Akakata ncha za matawi na kuzichukua hata nchi ya Kanaani; akaipanda katika
mji wa manahodha. 5 Pia akachukua mbegu ya nchi na kuipanda katika udongo
wenye rutuba. Akaiweka kando ya maji mengi kama mti umeao karibu na maji.
6 Kisha ukachipusha na mzabibu wenye kusambaa chini kwenye aridhi. Matawi
yake yakamwelekea yeye, na mizizi yake ikakua chini yake. Hivyo ukawa mzabibu
na kuzaa matawi na kutoa matawi. 7 Lakini kulikuwa na tai mwingine mkubwa
wenye mabawa makubwa na manyoya mengi. Tazama! Huu mzabibu ukabadilisha
mizizi yake kumwelekea tai, na ukasamabaza matawi yake kumwelekea tai kutoka
mahali ulipokuwa umepandwa basi upate kumwagiliwa. 8 Ulikuwa umepandwa
kwenye udongo mzuri kando ya maji mengi hivyo ungezaa matawi na kuanza kutoa
matunda, ili kuwa mzabibu mzuri kabisa.' 9 Waambie watu, 'Bwana Yahwe asema
hivi: Je! huo utafanikiwa? Je! Haitaing'oa mizizi yake na kuyakata matunda yake ili
kwamba unyauke, na majani yake yote mabichi yanyauke? Hakuna jeshi imara au
watu wengi watahitajika kuivuta kwa mizizi yake. 10 Basi tazama! Baada ya kuwa
umepandwa, je utakuwa? Je hautanyauka wakati upepo wa mashariki utakapoupiga?
Utanyauka kabisa katika kiwanja chake."' 11 Kisha neno la Yahwe likanijia, kusema,
12 "Waambie nyumba ya uasi, 'Je! hamjui haya mambo yana gana gani? Tazama!
Mfalme wa Babeli amekuja Yerusalemu na kumchukua mfalme wake na wakuu wake
na kuwaleta kwake mpaka Babebli. 13 Kisha akauchukua ukoo wa kifalme, akafanya
agano pamoja naye, na kumleta chini ya kiapo. Akawachukua watu wa nchi wenye
nguvu, 14 basi ufalme uwe duni na usijiinue wenyewe. Kwa kulitunza agano lake
nchi itaokoka. 15 Lakini mfalme wa Yerusalemu ameasi juu yake kwa kupeleka
mabalozi kwenda Misri ili kujipatia farasi na jeshi. Je! Atafanikiwa? Je! yeye
anayeyafanya haya mambo ataokoka? 16 Kama niishivyo! -hivi ndivyo Bwana Yahwe
asemavyo-atakufa hakika katika nchi ya mfalme aliyemfanya mfalme, yule mfalme
ambaye aliyekidharau kiapo chake, na ambaye aliyevunja agano lake. atakufa kati
ya Babeli. 17 Farao na jeshi lake lenye nguvu na kusanyiko la watu wengi kwa ajili
ya vita hawatamlinda katika vita, wakati jeshi la Wababeli watakapojenga tuta la
ngome na kuta za ngome ili kuyaharibu maisha ya wengi. 18 Kwa kuwa mfalme
amedharau kiapo chake kwa kulivunja agano. Tazama, ameunyoosha kwa mkono
wake ili kufanya ahadi na bado ameyafanya haya mambo yote. Hataokoka. 19 Kwa
hiyo Bwana Yahwe asema hivi: Kama niishivyo, Je! hiki hakikuwa kiapo changu
kwamba alidharau agano langu alilo livunja? Basi nitaleta nitamwadhibu juu ya
kichwa chake! 20 Nitausambaza wavu wangu juu yake, na atanaswa katika wavu
wangu wa kutegea. Kisha nitamleta hata Babeli na kuzitekeleza hukumu juu yake

huko kwa ajili ya uhaini wake alioufanya amenisaliti! 21 Wakimbizi wake wote katika
majeshi yake yataanguka kwa upanga, na wale watakaobakia watatawanyika kila
mahali. Kisha utajua yakwamba mimi ni Yahwe; nimesema hili litatokea." 22 Bwana
Yahwe asema hivi, 'Basi mimi mwenyewe nitaichukua sehemu ya juu ya mti wa
mkangazi, na nitaupanda mbali na matawi yake laini. Nitaukata, na mimi mwenyewe
nitaupanda juu ya mlima mrefu. 23 Nitaupanda juu ya milima ya Israeli hivyo utazaa
matawi na kuzaa matunda, na utakuwa mkangazi wa fahari ili kwamba kila ndege
arukaye ataishi chini ya huo. Watajenga viota chini ya kivuli cha matawi yake.
24 Kisha miti yote ya shambani itajua kwamba mimi ni Yahwe. Nimeishusha miti
mirefu na nimeiinua juu miti mifupi. Naunyausha mti mbichi na kuufanya mti
mkavu kuchanua. Mimi Yahwe, nimesema hivyo hii itatokea; nami nimelifanya hili.'"

# 18

1 Neno la Yahwe likanijia tena, kusema, 2 "Je mnamaana gani, ninyi mliotumia hii
mithali kuhusiana na nchi ya Israeli na kusema, 'Wababa wamekula zabibu mbichi,
na meno ya watoto imetiwa ganzi'? 3 Kama nishivyo-hivi ndivyo Bwana Yahwe
asemavyo-bila shaka hakutakuwa na fursa yoyote tena kwa ajili yenu kuitumia hii
mithali katika Israeli. 4 Tazama! Kila uhai ni mali yangu-uhai wa baba na uhai wa
mwana pia, ni mali yangu! roho itendayo dhambi ndiyo itakayokufa! 5 Itasemwaje
kuhusu mtu mwenye haki na achukuaye yaliyo halali na haki- 6 kama asipokula juu
ya milima au kuinua macho yake kwa sananmu za nyumba ya Israeli, na hakumnajisi
mke wa jirani yake, wala kumsemesha mwanamke katika kipindi chake cha mwezi,
je! Yu mwenye haki? 7 Je! Itasemwaje kuhusu mtu ambaye hakumkandamiza
yeyote, na kumrudisha mdeni wake kwa kile kilichokuwa kimewekwa kwa ajili ya
rehani, na hakuiba lakini kuwapatia chakula wenye njaa na kuwafunika uchi kwa
nguo, je yu mwenye haki? 8 Je! Itasemwaje kuhusu mtu ambaye hakuchukua faida
kubwa kwa ile pesa aliyokopa, na hakuchukua faida kubwa kwa kile alichokiuza?
9 Amesemwa kwamba amechukua yaliyo halali na kuimarisha uaminifu kati ya
watu. Kama huyo mtu akitembea katika sheria zangu na kuzishika hukumu zangu
kufanya kwa uaminifu, kisha ahadi kwa ajili ya mtu mwenye haki ni hii: Ataishi
hakika! -hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. 10 Lakini akizaa mwana mnyang'anyi
mmwaga damu na kufanya mengi katika haya mambo kama yalivyotajwa hapa,
11 hata kama baba yake hakufanya mojawapo katika haya mambo, lakini akala juu
ya milima na akamnajisi mke wa jirani yake, Je! itasemwaje juu yake? 12 Huyu
mtu huwakandamiza maskini na wahitaji, na huwakamata na kuwanyang'anya, na
hawarudishii dhamana, na huyanua macho yake kwa sanamu na kufanya matendo
maovu, 13 na hukopesha pesa kwa faida ya juu sana na kufanya faida kubwa juu ya
anachokiuza, Je! huyo mtu ataishi? Hakika hataishi! Atakufa hakika na damu yake
itakuwa juu yake kwa sababu amefanya haya mambo ya chuki. 14 Lakini Tazama!
tuseme kuna mtu aliyezaa mwana, na mwana wake huona dhambi zote za baba
yake alizozifanya, na kupitia kuziona, hakuyafanya hayo mambo. 15 Huyo mwana
hakula juu ya milima, na hakuinua macho yake kwa sanamu za nyumba ya Israeli,
na hakumtia unajisi mke wa jirani yake, Je! itasemwaje juu yake? 16 Yule mwana
hakumkandamiza yeyote, au kutwaa dhamana, au kupoteza vitu, lakini badala yake
kutoa chakula chake kwa wenye njaa na kuwafunika wenye uchi kwa nguo. 17 Huyo
mwana hakumkandamiza yeyote au au kuchukua faida ambayo ni ya juu sana au
kufanya manufaa kwa ajili ya mkopo, lakini ameyashika maagizo yangu na kuenenda
sawa sawa na sheria zangu; huyo mwana hatakufa kwa ajili ya dhambi za baba
yake: Ataishi hakika! 18 Baba yake, kwa kuwa aliwakandamiza wengine kwa nguvu
nyingi na kumnyang'anya ndugu yake, na kufanya yasiyo mema miongoni mwa

watu wake-tazama, atakufa katika uovu wake. [19] Lakini ninyi husema, 'Kwa nini
mwana asibebe uovu wa baba yake?' Kwa sababu mwana hubeba yaliyo halali na
haki na kuzitunza amri zangu; huzifanya. Ataishi hakika! [20] Yule atendaye dhambi,
ndiye ambaye atakufa. Mwana hatabeba uovu wa baba yake, na baba hatabeba
uovu wa mwana wake. Haki ya yule atendaye haki itakuwa juu yakwe mwenyewe,
na uovu wa mwenye uovu utakuwa juu yake mwenyewe. [21] Lakini kama mwovu
ageukapo kutoka dhambi zake zote alizofanya, na kuzitunza sheria zangu zote na
kufanya yaliyo halali na haki, kisha hakika ataishi na hatakufa. [22] Makosa yote
aliyoyafanya hayatakumbukwa juu yake. Ataishi kwa hiyo haki aliyoitenda. [23] Je!
Nitafurahia juu ya kifo cha mwovu-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-na sio katika
kugeuka kwake kutoka njia yake ili kwamba aweze kuishi? [24] Lakini kama mtu
mwenye haki ageukapo kutoka kwenye haki yake na kufanya maovu na kutenda
machukizo kama machukizo yote ambayo mtu mwovu afanyayo, basi ataishi? Haki
yake yote aliyoifanya haitakumbukwa wakati atakaponisaliti katika uhaini wake.
Hivyo atakufa katika dhambi alizofanya. [25] Lakini ninyi husema, 'Njia ya Bwana
si sawa!' sikilizeni, nyumba ya Israeli! Je njia zangu haziko sawa? Je si njia ambazo
haziko sawa? [26] Wakati mtu mwenye haki ageukapo kutoka kwenye makosa yake,
na kufanya maovu na kufa kwa sababu ya hayo, kisha atakufa katika uovu ambao
alioufanya. [27] Lakini wakati mtu mwovu ageukapo kutoka uovu wake alioufanya
na kufanya yaliyo halali na haki, kisha ataulinda uhai wake. [28] Kwa kuwa ameona
na kugeuka kutokana na makosa yake yote ambayo aliyoyafanya. Hakika ataishi, na
hatakufa. [29] Lakini nyumba ya Israeli husema, 'Njia ya Bwana haiko sawa!' Ni namna
gani njia zangu si sawa, nyumba ya Israeli? Ni njia zenu ndizo si sawa. [30] Kwa hiyo
nitamuhukumu kila mtu miongoni mwenu kulingana na njia zake, nyumba ya Israeli!
-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. Tubuni na rudini kutoka kwenye makosa yenu
yote ili kwamba wasiwe kikwazo cha uovu dhidi yenu. [31] Tupilia mbali makosa yenu
yote mliyoyafanya; jifanyieni moyo mpya na roho mpya. Kwa nini mfe, nyumba
ya Israeli? [32] Kwa kuwa sifurahii kifo cha yule afaye-hivi ndivyo Bwana Yahwe
asemavyo-hivyo tubuni na muishi!”

# 19

[1] “Tena wewe, chukua maombolezo juu ya viongozi wa Israeli [2] na sema, 'Mama
yako alikuwa nani? Simba jike mmoja, aliishi na mtoto wa simba dume; katikati ya
simba wadogo, aliwalisha watoto wake. [3] Alimlea mmoja wa wale watoto kurarua
wanyama wengine, na kisha alijifunza jinsi ya kuwinda watu na kuwala. [4] Kisha
mataifa wakasikia kuhusu yeye. Akakamatwa kwenye mtego wao, na wakamleta
kwa kulabu hata nchi ya Misri. [5] Kisha alipoona kwamba ingawa alikuwa akimsubiri
arudi, matumaini yake sasa yalienda, hivyo alimchukua mtoto wake wengine katika
watoto wake na kumlea hata kuwa mwana simba. [6] Huyu mwana simba alitembea
huku na huku katikati ya simba. Akawa mwana simba na kujifunza kuwinda
mawindo; akala watu. [7] Akawakamata wajane na kuiharibu miji. Nchi na viijazavyo
vilitelekezwa kwa sababu ya sauti ya kunguruma kwake. [8] Lakini mataifa yakaja
juu yake kutoka mikoa yote; wakatengeneza nyavu juu yake. Akakamatwa kwenye
mtego wao. [9] Kwa kulabu wakamuweka kwenye tundu na kisha wakamleta hata
kwa mfalme wa Babeli. Wakamleta hata kwenye ngome imara ili kwamba sauti yake
isiweze kusikika juu ya milima ya Israeli. [10] Mama yako alikuwa kama mzabibu
uliopandwa kwenye damu yako karibu na maji. ulizaa matunda na kujaa matawi
kwa sababu ya wingi wa maji. [11] Ulikuwa na matawi imara yaliyokuwa yakitumika
kwa ajili ya fimbo ya utawala, na kipimo chake kiliinuka juu ya matawi, na kina
wake ulionekana kwa ukubwa wa majani yake. [12] Lakini mzabibu uling'olewa kwa

ghadhabu na kutupwa chini hata aridhini, na upepo wa mashariki uliuvunja na
kunyauka na moto ukavila. 13 Hivyo sasa, umepandwa jangwani, kwenye nchi ya
ukame na kavu. 14 Kwa kuwa moto ulitoka kwenye matawi makubwa na kuyala
matunda yake. Hakuna tawi imara juu yake, hakuna fimbo ya kifalme kutawala.'
Haya ni maombolezo na yataimbwa kama maombolezo."

# 20

1 Ikawa ikaja katika mwaka wa saba, siku ya kumi ya mwezi wa tano, wazee wa
Israeli wakaja kumuuliza Yahwe na kuketi mbele yangu. 2 Kisha neno la Yahwe likani-
jia, kusema, 3 "mwanadamu, tangaza kwa wazee wa Israeli na uwaambie, 'Bwana
Yahwe asema hivi: Je! Mmekuja kuniuliza swali? Kama niishivyo, sitaulizwa swali na
ninyi! -hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo.' 4 Je! Utawahukumu? Utamuhukumu,
mwanadamu? Wajulishe kuhusu machukizo ya baba zao. 5 Waambie, 'Bwana Yahwe
asema hivi: Katika siku niliyoichagua Israeli na kuinua mkono wangu kuapa kiapo
kwa uzao wa nyumba ya Yakobo, na kufanya kujulikana mimi mwenyewe kwao
katika nchi ya Misri, wakati nilipoinua mkono wangu kuapa kiapo kwao. Nalisema,
"Mimi ni Yahwe Mungu wenu"- 6 siku hiyo niliinua mkono wangu kuapa kiapo kwa
ajili yao kwamba nitawatoa kutoka nchi ya Misri kwenye nchi ambayo niliyokuwa
nimeichagua kwa umakini kwa ajili yao. Ilikuwa ikitiririka maziwa na asali; ilikuwa
nzuri sana utukufu miongoni mwa nchi mbali mbali. 7 Nikawaambia, "Kila mtu
atupilie mabli mambo ya machukizo kutoka mbele ya macho yake na sanamu za
Misri. Msijitie unajisi; mimi ni Yahwe Mungu wenu." 8 Lakini wameasi juu yangu
hawakuwa tayari kunisikiliza. Kila mtu hakutupilia mbali mambo ya machukizo
kutoka mbele ya macho yake wala kwa ajili ya sanamu za Misri, hivyo nikaona
nimwage ghadhabu yangu juu yao kukamilisha hasira yangu miongoni mwao katikati
ya nchi ya Misri. 9 Nilifanya kwa ajili ya jina langu ili lisinajisiwe katika macho
ya mataifa ambao walikaa pamoja nao. Nilijifanya mwenyewe kujulikana kwao,
katika macho yao, kwa kuwatoa katika nchi ya Misri. 10 Basi nikawatoa katika nchi
ya Misri na kuwaleta kwenye jangwa. 11 Kisha nikawapa amri zangu na kufanya
maagizo yangu kujulikana kwao, kwa kila mwanadamu atakayezishika ataishi. 12 Pia
nikawapatia Sabato zangu kama ishara kati yangu na wao, ili wajue kwamba mimi
ni Yahwe niwafanyao wawe watakatifu. 13 Lakini nyumba ya Israeli imeasi dhidi
yangu jangwani. Hawakuenenda katika amri zangu; badala yake, wameyakataa
maagizo yangu, ambayo mwanadamu ataishi kama akiyatii. Wamezinajisi Sabato
zangu sana, basi nikasema nitamwaga hasira yangu juu yao jangwani ili kuwamalliza.
14 Lakini nilifanya kwa ajili ya jina langu hivyo lisinajisiwe katika macho ya mataifa,
ambao niliwatoa mbele ya macho yao kutoka Misri. 15 Basi mimi mwenyewe pia
nimeinua mkono wangu kuapa kiapo kwao jangwani sitawarudisha kwenye nchi ile
niliyokuwa naenda kuwapatia, nchi inayotiririkayo maziwa na asali, ambayo ilikuwa
nzuri sana ambayo ni nzuri kati ya nchi zote. 16 Nimeapa hivi kwa sababu walikataa
maagizo yangu na kutotembea katika amri zangu, na wazikufuru Sabato zangu.
17 Lakini jicho langu likawahurumia kutokana na uharibifu na sikuwaangamiza
jangwani. 18 Nikawaambia watoto wao jangwani, "Msitembee kutokana na amri za
wazazi wenu; msiweke maagizo yao au kujinajisi wenyewe kwa sanamu. 19 Mimi
ni Yahwe Mungu wenu, tembeeni katika amri zangu; tunzeni maagizo yangu na
kuyatii. 20 Zitunzeni Sabato zangu takatifu ili kwamba zitakuwa ishara kati yangu
na ninyi, hivyo basi mtajua yakwamba mimi ni Yahwe Mungu wenu." 21 Lakini
watoto wao waliniasi. Hawakutembea kwenye sheria zangu au kushika maagizo
yangu, ambazo mwanadamu ataishi kama akizitii. Wamezinajisi Sabato zangu, hivyo
nimeamua kumwaga ghadhabu yangu juu yao kutimiza ghadhabu yangu dhidi yao

katika jangwa. [22] Lakini niliurudisha mkono wangu na kutenda kwa ajili ya jina
langu, hivyo lisitiwe unajisi katika macho ya mataifa ambao mbele ya macho yao
niliwatoa Waisraeli. [23] Mimi mwenyewe pia nimeuinua mkono wangu kuapa juu
yao jangwani, kwamba nitawatawanya kati ya maifa na kuwatawanya miongoni
mwa nchi mabali mbali. [24] Nimeamua kufanya hivi kwa kuwa hawakuzitii amri
zangu, na tangu walipo zikataa sheria zangu na kuzinajisi Sabato zangu. Macho
yao yalizitamani sanamu za baba zao. [25] Kisha niliwapa amri ambazo hazikuwa
nzuri, na maagizo ambayo hawakuweza kuishi kwayo. [26] Nikawafanya unajisi
kwa zawadi zao wakati walipofanya dhabihu za kila limbuko la tumbo la uzazi
na kutupa kwenye moto. Nalifanya hivi ili kuwaogofya hivyo wangeweza kujua
kwamba mimi ni Yahwe!' [27] Kwa hiyo, mwanadamu, waambie nyumba ya Israeli na
waambie, 'Bwana Yahwe asema hivi: Katika hili pia baba zenu walinikufuru wakati
walipokuwa sio waaminifu kwangu. [28] Wakati nilipowaleta kwenye nchi ambayo
niliyokuwa nimewaapia kuwapatia, na kisha popote walipoona jiwe lolote refu na
mti wenye majani, walitoa sadaka zao, walinikasirisha kwa sadaka zao, na huko pia
walichoma ubani wao wa kunukia na kumwaga sadaka zao za kinywaji. [29] Kisha
nikawaambia, "Nini maana ya mahali palipoinuka ambapo mmeleta sadaka huko?"
Hivyo jina lake linaitwa Bana hata leo.' [30] Kwa hiyo waambie nyumba ya Israeli,
'Bwana Yahwe asema hivi: Je! Kwa nini unajinajisi mwenyewe kwa njia za baba
zako? Kwahiyo kwa nini unatenda kama makahaba, kutafuta kwa ajili ya mambo
ya machukizo? [31] Kwa kuwa wakati mtoapo zawadi zenu na kuwaweka watoto
wenu kwenye moto, siku hii mnajitia unajisi pamoja na sanamu zenu zote. Kwa hiyo
kwa nini niwaache mniulize mimi, nyumba ya Israeli? Kama niishivyo-Hivi ndivyo
Bwana Yahwe asemavyo-Sitawaacha mniulize swali. [32] Mawazo yanayoumbika
kwenye moyo wako hayatatokea kamwe. Mmesema, "Ngoja tuwe kama mataifa
mengine, kama koo za nchi nyingine waabuduo mti na jiwe." [33] Kama niishivyo-
hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-Nitatawala hakika juu yenu kwa mkono wenye
nguvu, mkono ulionyooshwa, na ghadhabu itakayomwagwa juu yenu. [34] Nitawatoa
kutoka kwa watu wengine na kuwakusanya kutoka kwenye nchi mlizotawanyika
ndani mwao. Nitafanya hivi kwa mkono hodari na kwa ghadhabu iliyomwagika.
[35] Kisha nitawaleta kwenye jangwa la watu, na huko nitawahukumu uso kwa uso.
[36] Kama nilivyo wahukumu baba zenu katika jangwa la nchi ya Misri, hivyo pia
nitawahukumu-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. [37] Nitawafanya mpite chini ya
fimbo yangu, na nitawafanya kutii maagizo yangu ya agano. [38] Nitawasafisha kutoka
miongoni mwenu maasi na wale ambao walionichukiza. Nitawatoa kutoka nchi
ambayo wanayoishi kama wageni, lakini hawataingia kwenye nchi ya Israeli. Kisha
mtajua yakwamba mimi ni Yahwe. [39] Basi kwenu, nyumba ya Israeli, Bwana Yahwe
asema hivi: Kila mmoja wenu ataenda kwa sanamu zake mwenyewe. Muwaabudu
kama mtakataa kunisikiliza, lakini hamtalikufuru tena jina langu takatifu kwa
zawadi zenu na sanamu zenu. [40] Kwa kuwa juu ya mlima wangu mtakatifu,
juu ya kilele cha mlima wa Israeli-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-wote wa
nyumba ya Israeli mtaniabudu huko katika nchi. Nitabarikiwa kwa kutaka sadaka
zenu huko, na pia malimbuko yenu ya shukrani pamoja na vitu vyenu vyote
vitakatifu. [41] Nitawapokea kama harufu nzuri ya ubani wakati nitakapowatoa kutoka
wale watu na kuwakusanya toka nchi ambazo mlizotawanyika. Nitajifunua mimi
mwenyewe kama mtakatifu ndani yenu kwa ajili ya mataifa waone. [42] Kisha,
wakati nitakapowaleta katika nchi ya Israeli, kwenye nchi ambayo niliuinulia mkono
wangu kuapa kuwapatia baba zenu, mtajua yakwamba mimi ni Yahwe. [43] Kisha
mtazikumbuka njia zenu mbaya huko, na matendo yenu yote machafu mliyoyafanya
wenyewe, na mtajichukia wenyewe katika macho yenu kwa matendo yenu yote

maovu mliyoyafanya. 44 Hivyo mtajua kwamba mimi ni Yahwe nifanyapo haya
kwenu kwa ajili ya jina langu, sio kwa njia zenu mbaya au matendo yenu mabovu,
nyumba ya Israeli-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo."' 45 Kisha neno la Yahwe
likanijia, kusema, 46 "Mwanadamu, weka uso wako kuelekea nchi za kusini, na
kuongea juu ya kusini; tabiri juu ya msitu wa Negebu. 47 Uuambie msitu wa Negebu,
'Hivi ndivyo Yahwe asemavyo-Bwana Yahwe asema hivi: Tazama, nitaweka moto
ndani yako. Utakula kila mti mbichi na kila mti mkavu ndani yako. Miali ya
moto haitazimika; na kila uso utokao kusini hata kaskazini utateketezwa kwa moto.
48 Kisha watu wote wenye mwili watajua yakwamba mimi ni Yahwe nimeuwasha
moto, na hautazimika."' 49 Kisha nimesema, Ee! Bwana Yahwe, Wananisema mimi,
'Je! yeye sio mwenye kusema mafumbo?"'

# 21

1 Kisha neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 "Mwanadamu, weka uso wako kuelekea
Yerusalemu, na neno juu ya patakatifu; tabiri juu ya nchi ya Israeli. 3 Sema juu ya nchi
ya Israeli, 'Yahwe asema hivi: Tazama! Ni juu yako! Nitautoa upanga wangu kutoka
kwenye ala yake na kuwakatilia mbali wote yaani mtu mwenye haki na mtu mwovu
kutoka kwako! 4 Ili niwakatilie mbali wote, mwenye haki na mwovu kutoka kwako,
upanga wangu utatoka kwenye ala yake juu ya wote wenye mwili kutoka kusini hata
kaskazini. 5 Kisha wote wenye mwili watajua yakwamba mimi, Yahwe, nimeutoa
upanga wangu kutoka kwenye ala yake. Hautarudi tena!' 6 Kwa hiyo, mwanadamu,
gumia kama kuvunjika kwa viuno vyako! Katika uchungu gumia mbele ya macho
yao! 7 Kisha itatokea kwamba watakuuliza, 'Kwa sababu gani unalia?' Kisha utasema,
'Kwa sababu ya habari inayokuja, kwa kuwa kila moyo utakuwa dhaifu, na kila
mkono utasita! Kila roho itazimia, na kila goti litatiririrka kama maji. Tazama!
Inakuja na itakuwa kama hivi! -hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo."' 8 Kisha neno
la Yahwe likanijia, kusema, 9 "Mwanadamu, tabiri na sema, 'Bwana asema hivi: sema:
Upanga! Upanga! Utachongwa na kusuguliwa! 10 Utanolewa ili kushiriki katika
machinjio makubwa! Utasuguliwa ili uwe kama mng'ao wa radi! Je! Tufanye furaha
katika fimbo ya mwana wa mfalme? Upanga ujao huchukia kila hiyo fimbo! 11 Hivyo
upanga utatolewa kwa ajili ya kusuguliwa, na kisha kushikika kwa mkono! Upanga
umechongwa na umesuguliwa na utatolewa kwenye mkono wa yule auaye!' 12 Ita
msaada na omboleza, mwanadamu! Kwa kuwa upanga umekuja juu ya watu wangu!
Uko juu ya wakuu wote wa Israeli. Wametolewa dhidi ya upanga pamoja na watu
wangu. Kwa hiyo, piga paja lako! 13 Kwa kuwa kuna kujaribiwa, lakini itakuwaje
kama fimbo ya kifalme haitakuwepo tena? -hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo.
14 Basi wewe, mwanadamu, tabiri, na piga makofi, kwa kuwa upanga utakushambulia
hata mara tatu! Upanga kwa wale watakaochinjwa! Utakuwa upanga kwa ajili
ya kuchinjia, ukiwatoboa pande zote! 15 Ili kuyeyusha mioyo yao na kuongeza
kuanguka kwao, nimeweka machinjio ya upanga juu ya malango! Ole! Umeundwa
kama mng'ao wa radi, umetengwa kwa ajili ya kuua! 16 Wewe, upanga! Nyooka
upande wa kuume! Nyooka upande wa kushoto! Nenda popote ulipoelekeza uso
wako. 17 Kwa kuwa pia nitapiga mikono yangu miwili kwa pamoja (makofi), na kisha
nitaleta ghadhabu yangu kwa waliobakia! Mimi, Yahwe, nimesema hivi!" 18 Neno la
Yahwe likanijia tena, kusema, 19 "Sasa wewe, mwanadamu, teua njia mbili kwa ajili
ya upanga wa mfalme wa Babeli upate kuja. Njia hizo mbili zitaanza katika nchi moja,
na kibao cha barabarani kitamwonyesha mmoja wao kama kuuelekea mji. 20 Onyesha
njia moja kwa ajili ya jeshi la Wababeli kuja Raba, mji wa Waamoni. Onyesha
nyingine kuelekea jeshi la Yuda na mji wa Yerusalemu, ambayo imeimarishwa.
21 Kwa kuwa mfalme wa Babeli atasimama kwenye makutano ya barabara, kwenye

njia panda, ili kufanya uganga. Alitingisha mishale na kuuliza mwelekeo kutoka kwa
sanamu na atalichunguza ini. 22 Katika mkono wake wa kuume kutakuwa na dalili
kuhusu Yerusalemu, kuweka mitambo ya kubomolea juu ya hiyo, kufungua kinywa
chake kupanga kuchinja, kutoa sauti ya vita, kuweka mitambo ya kubomolea juu
ya malango, kujenga ngazi, na kusimamisha wima minara ya boma. 23 Itaonekana
kuwa ishara isiyofaa katika macho ya wale walio katika Yerusalemu, wale walioapa
kiapo kwa Wababeli! Lakini mfalme atawashtaki kwa kuvunja sheria ya mkataba ili
kuwabariki! 24 Kwa hiyo Bwana Yahwe asema hivi: Kwa sababu umeuleta uovu wako
kwenye kumbukumbu zangu, makosa yenu yatafunuliwa! Dhambi zenu zitaonekana
katika matendo yenu yote! Kwa sababu hii utamkumbusha kila mtu mtakamatwa
kwa mkono wa adui yenu! 25 Kama wewe, mchafu na mtawala mwovu wa Israeli,
ambaye siku ya hukumu imekuja, na ambaye mda wa kufanya uovu umekoma,
26 Bwana Yahwe asema hivi kwako: Toa kilemba na vua taji! Mambo hayatakuwa
tena kama yalivyokuwa! Kiinue kilicho chini na kiinue kilichoinuka! 27 Uharibifu!
Uharibifu! Nitaiharibu! Haitakuwa tena hadi atakapokuja yeye ambaye ameteuliwa
kutekeleza hukumu. 28 Basi wewe, mwanadamu, tabiri na sema, 'Bwana Yahwe
asema hivi hawa ni watu wa Amoni kuhusiana na ujio wa aibu yao: Upanga, upanga
umechirwa! Umenolewa kwa ajili ya kuchinja, hivyo utakuwa kama kimuli muli cha
radi! 29 Wakati manabii wameona maono ya uongo juu yako, wakati watakapofanya
matambiko kuuijia kwa uongo juu yako, huu upanga utaanguka chini juu ya shingo
za mwovu ambao wako karibu kuuawa, ambao siku ya ghadhabu imekuja na ambao
mda wa uovu unakaribia kuisha. 30 Rudisha upanga kwenye gala yake. Katika mahali
ulipoumbwa, katika nchi ya chimbuko lako, nitakuhukumu! 31 Nitamwaga hasira
yangu juu yako! Nitapuliza upepo wa moto wa ghadhabu juu yako na kukuweka
kwenye mkono wa watu wakatili, watu wajuao kuangamiza! 32 Utakuwa kuni kwa
ajili ya moto! Damu yako itakuwa kati ya nchi. Hutakumbukwa tena, kwa kuwa
mimi, Yahwe nimesema hivi!"'

## 22

1 Kisha neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 "Sasa wewe, mwanadamu, Je!
Utanihukumu? Utauhukumu mji kwa damu? Mfanye ajue machukizo yake yote.
3 Utasema, 'Bwana Yahwe asema hivi: Huu ndiyo mji umbao umwagao damu kati
yake ili kwamba mda wake ufike; mji ufanyao sanamu ili ujitie unajisi. 4 Umekuwa
na hatia kwa damu uliyoimwaga, na kufanya unajisi kwa sanamu ulizozitengeneza.
Kwa kuwa umezileta karibu siku zako na kuzikaribia siku zako za mwisho. Kwa
hiyo nitakufanya lawama kwa mataifa na kejeli katika uso wa kila nchi. 5 Wote
walio karibu na wale walio mbali nawe watakudhihaki, wewe mji mchafu, ujulikanao
kila mahali kwa sifa mbaya kama kujaa machafuko. 6 Tazama! Wakuu wa Israeli,
kila mmoja kwa nguvu yake, wamekuja kwako kumwaga damu. 7 Wamefanya
udanganyifu kwa baba na mama ndani yako, na wametenda yaliyo kinyume juu
ya wageni kati yako. Wamewatenda vibaya yatima na wajane ndani mwako.
8 Umevidharau vitu vyangu vitakatifu na kuinajisi Sabato yangu. 9 Watu wasingiziaji
wamekuja kati yako ili kumwaga damu, na hula juu ya milima. Hufanya uovu
kati yako. 10 Uchi wa baba umefunuliwa ndani yako. Wamemtukana mwanamke
mchafu ndani yako wakati wa uchafu wake. 11 Watu waliofanya machukizo pamoja
na wake za majirani zao, na watu wafanyao uchafu wa aibu kwa mke wa mwanao
mwenyewe; watu wawatukanao dada zao wenyewe-binti za baba zao wenyewe-
haya yote yapo miongoni mwanu. 12 Hawa watu huchukua rushwa kati yenu ili
kumwaga damu. Umechukua faida na kuongeza riba nyingi sana, na umenisahau-
hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. 13 Tazama! Kwa mkono wangu nimeipiga faida

ambayo uliyoitengeneza kwa njia isiyo halali, na damu iliyo kati yako. 14 Je! Moyo
wako utasimama, mikono yako itakuwa hodari katika siku wakati mimi mwenyewe
nitakapo kushughulikia? Mimi, Yahwe, nasema hivi, na nitalifanya. 15 Hivyo
nitakutawanya kati ya mataifa na kukutawanya kati ya nchi mbali mbali. Katika
njia hii, nitausafisha uchafu kutoka kwako. 16 Hivyo utakuwa mchafu machoni mwa
mataifa. Kisha utajua kwamba mimi ni Yahwe."' 17 Kisha neno la Yahwe likanijia,
kusema, 18 "Mwanadamu, nyumba ya Israeli imekuwa takataka kwangu. Wote
wamekuwa masazo ya shaba na bati, na chuma na risasi kati yenu. Watakuwa kama
takataka ya fedha katika tanuu. 19 Kwa hiyo Bwana Yahwe asema hivi, 'Kwa sababu
mmekuwa kama takataka, kwa hiyo, tazama! Nataka kuwakusanya katikakati ya
mji wa Yerusalemu. 20 Kama kukusanya fedha na shaba, chuma, risasi na chuma
kati ya tanuu ili kuvifukutia moto na kuviyeyusha juu yake, nitawayeyusha. Hivyo
nitawakusanya katika hasira yangu na ghadhabu. Nitawaweka hapo na kufukutisha
moto juu yake ili kuiyeyusha; hivyo nitawakusanya katika hasira yangu na ghadhabu
yangu, na nitawaweka hapo na kuwayeyusha. 21 Basi nitawakusanya na kuwafukutia
kwa moto wa hasira yangu juu yenu hivyo basi mtamwagwa kati yake. 22 Kama
kuyeyusha fedha kati ya tanuu, mtayeyushwa chini kati yake, na mtajua yakwamba
mimi, Yahwe, nimemwaga ghdhabu yangu juu yenu!"' 23 Neno la Yahwe likanijia,
kusema, 24 "Mwanadamu, mwambie, 'Wewe ni nchi ambayo haijasafishwa. Hakuna
mvua siku ya hasira! 25 Kuna njama ya manabii wake kati yake, kama simba
angurumaye akirarua mawindo. Wamekula uhai na kuchukua utajiri wa thamani;
wamewafanya wajane wengi ndani yake! 26 Makuhani wake hufanya kinyume na
sheria yangu, na wamevinajisi vitu vyangu vitakatifu. Hawawezi kutofautisha kati
ya vitu vitakatifu na vitu vya najisi. Wanaficha macho yao kutoka Sabato zangu
hivyo basi nimetiwa unajisi kati yao. 27 Wakuu wake ndani mwake wamekuwa
kama mbwa mwitu wakirarua mawindo yao. Wamemwaga damu na kuharibu
maisha, ili kupata faida kwa njia ya udanganyifu. 28 Manabii wake wamepakwa
chokaa; wanaona maono ya uongo na kutabiri uongo kwao. Wanasema "Bwana
Yahwe asema hivi"' wakati Yahwe hajanena. 29 Watu wa nchi wamewakandamiza
kwa kutaka kwa nguvu na kuwanyang'anya kwa nguvu, na wamewatesa maskini na
wahitaji, na kuwakandamiza wageni bila haki. 30 Hivyo nimetafuta mtu kutoka kwao
ambaye ataweza kujenga ukuta na ambaye atakayeweza kusimama mbele yangu
katika uvunjaji wake kwa ajili ya nchi basi sitaweza kuiharibu, lakini sikuona mtu.
31 Hivyo nitaimwaga ghadhabu yangu juu yao. Nitawamaliza kwa moto wa ghadhabu
yangu na kuweka njia yao juu ya vichwa vyao wenyewe-hivi ndivyo Bwana Yahwe
asemavyo."'

# 23

1 Neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 "Mwanadamu, Kulikuwa na wanawake wawili,
binti za mama mmoja. 3 Walifanya ukahaba katika Misri katika kipindi cha ujana
wao. Walitenda kama makahaba huko. Maziwa yao yalikuwa yamebana na ubikira
wa chuchu zao zilipapaswa huko. 4 Majina yao yalikuwa Ohola-dada mkubwa-na
Oholiba-dada yake mdogo. Kisha wakawa wangu na kuzaa wana na binti. Majina
yao yalikuwa yakimaanasha hivi: Ohola maana yake Samaria, na Oholiba maana
yake Yerusalemu. 5 Lakini Ohola alifanya kama kahaba hata alipokuwa wangu;
aliwatamani wapenzi wake, kwa kuwa Waashuri na nguvu, 6 liwali aliyekuwa
amevaa urijuana, na kwa ajili ya maafisa wake, waliokuwa hodari na wanaume
wa kuvutia, wote walikuwa waendesha farasi. 7 Hivyo akajitoa yeye mwenyewe
kama kahaba kwao, kwa watu bora wa Ashuru, na alijitia mwenyewe uchafu
pamoja na kila mmoja aliyekuwa amemtamani-pamoja na sanamu zake zote. 8 Kwa

kuwa hakuacha tabia zake za kihaba nyuma katika Misri, wakati walipolala naye
wakati alipokuwa msichana mdogo, wakati walipoanza kwanza kupapasa ubikira
wa maziwa yake, wakati walipoanza kummwagia tabia ya uzinzi wao juu yake.
9 Kwa hiyo nilimtia kwenye mkono wa wapenzi wake, kwenye mkono wa Waashuru
kwa kuwa aliwatamani. 10 Wakamfunua uchi wake. Wakawachukua wana wake
na binti, na wakamuua kwa upanga, na akawa aibu kwa wanawake wengine, hivyo
wakapitisha hukumu juu yake. 11 Dada yake Oholiba akaliona hili, lakini aliyatamani
zaidi na kufanya kama kahaba hata zaidi kuliko dada yake. 12 Aliwatamanai
Waashuru, mabosi na watawala waliokuwa wamevaa ngua za ushawishi, walikuwa
watu waendesha farasi. Wote walikuwa hodari, wote vijana wa kuvutia. 13 Nikaona
kwamba alikuwa amefanya uchafu mwenyewe. Ilikuwa kama kwa wadada wote.
14 Kisha akaongeza ukahaba wake tena zaidi. Aliona watu waume waliokuwa
wamechorwa juu ya kuta, michoro ya Wakaldayo iliyochorwa kwa rangi nyekundu,
15 waliovaa mikanda kuzunguka viuno vyao, na vilemba virefu juu ya vichwa vyao.
Wote walikuwa na mwonekano wa maafisa wa jeshi la waendesha farasi, mfano
wa wana wa Wababeli, ambao asili ya nchi ni Ukaldayo. 16 Na mara macho yake
yalipowaona, aliwatamani, hivyo akawatuma wajumbe wake kwao katika Ukaldayo.
17 Kisha Wababeli wakaja katika kitanda chake cha tamaa, na walimfanya unajisi
kwa uzinzi wao. Kwa kile alichokuwa amekifanya alifanya unajisi, basi akageuka
mwenyewe kutoka kwao katika karaha. 18 Alionyesha matendo yake ya ukahaba
na alionyesha uchi wake, hivyo roho yangu ikagauka kutoka kwake, kama roho
yangu ilivyogeuka kutoka kwa dada yake. 19 Kisha alifanya matendo mengi zaidi
ya ukahaba, akakumbuka na kutafakari siku za ujana wake, wakati alipotenda kama
kahaba katika nchi ya Misri. 20 Basi akawatamani wapenzi wake, ambao sehemu zao
za siri zilikuwa kama zile za punda, na kile kizaliwacho hutoka kilikuwa kama wale
farasi. 21 Hivi ndivyo ulivyofanya matendo ya aibu ya ujana wako, wakati Wamisri
walipopapasa chuchu zako kuyaminya maziwa ya ujana wako. 22 Kwa hiyo, Oholiba,
Bwana Yahwe asema hivi, 'Tazama! Nitawarudisha wapenzi wako dhidi yako. Wale
ambao uliowarudisha, nitawaleta juu yako kutoka kila upande. 23 Wababeli na
Wakaldayo wote, Pekodi, Shoa, na Koa, na Waashuru wote pamoja nao, hodari, vijana
wa kutamanika, magavana na maamiri jeshi, wote ni maafisa na watu wote wenye
sifa, wote wenye kuendesha farasi. 24 Watakuja juu yako kwa silaha, na kwa magari
ya farasi na mikokoteni, na kundi kubwa la watu. Watapanga ngao kubwa, ngao
ndogo, na kofia za chuma juu yako pande zote. Nitawapatia nafasi kukuadhibu, na
watakuadhibu kwa matendo yao. 25 Kwa kuwa nitaweka hasira yangu ya wivu juu
yako, na watashughulika na wewe kwa hasira. Watakukatilia mbali pua zako na
masikio yako, na masalia yako wataanguka kwa upanga. Watawachukua wana wako
na binti zako, na masalia yako watateketea kwa moto. 26 Watakuvua nguo zako na
kuchukua mapambo yako ya vito. 27 Hivyo nitaiondoa tabia yako ya aibu kutoka
kwako na matendo yako ya kikahaba kutoka nchi ya Misri. Hutainua macho yako
kuwaelekea kwa sahauku, na hutaikumbuka Misri tena.' 28 Kwa kuwa Bwana Yahwe
asema hivi, 'Tazama! Nitakutia katika mkono wa wale uwachukiao, kukurudisha
kwenye mkono wa wale ambao uliokuwa umewarudisha. 29 Watashughulika pamoja
nawe kwa chuki; watachukua milki zako zote na kukutelekeza uchi na kukuweka
wazi. Uchi wa aibu ya ukahaba wako utafunuliwa, tabia yako ya aibu na uzinzi
wako. 30 Haya mambo yatafanyika kwako kwa kuwa umetenda kama kahaba, tamaa
za mataifa kwazo umetiwa unajisi kwa sanamu zao. 31 Umetembea katika njia
za dada yako, hivyo nitaweka kikombe chake cha adhabu kwenye mkono wako.'
32 Bwana Yahwe asema hivi, 'Utakinywea kikombe cha dada yako ambacho ni kirefu
na kikubwa. Utakuwa dhihaka na kutawaliwa na dharau-hiki kikombe kimejaa kiasi

kikubwa. [33] Utajazwa kwa ulevi na huzuni, kikombe cha ushangao na uharibifu;
kikombe cha dada yako Samaria. [34] Utakinywea na kubakia kitupu; kisha utakivunja
vunja na kuyararua maziwa yako kuwa vipande vipande. Kwa kuwa nimesema
hivyo-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo.' [35] Kwa hiyo, Bwana Yahwe asema hivi,
'Kwa sababu umenisahau na kunitupa mbali nyumba ya mgongo wako, basi pia
utachukua matokeo ya tabia zako za aibu na matendo ya uasherati.”' [36] Yahwe
akanambia, “Mwanadamu, Je! utamhukumu Ohola na Oholiba? Basi waambie
matendo yao ya machukizo, [37] kwa kuwa wamefanya uzinzi, na kwa kuwa kuna damu
juu ya vichwa vyao. Wamefanya uzinzi na sanamu zao, na wamewaweka hata wana
wao kwenye moto, kama chakula cha sanamu zao. [38] Kisha waliendelea kufanya hivi
kwa ajili yangu: Wamepafanya patakatifu pangu unajisi, na katika siku hiyo hiyo
wakainajisi Sabato zangu. [39] Kwa kuwa walipokuwa wamewachinjia watoto wao kwa
ajili ya sanamu zao, kisha wakaja hata patakatifu pangu siku hiyo hiyo kupanajisi!
Hivyo tazama! Hivi ndivyo walivyofanya kati ya nyumba yangu. [40] Mmewatuma
watu kutoka mbali, ambao wajumbe waliwatuma-sasa tazama. Wakaja kweli, ambao
uliojiosha kwa ajili yao, uliweka rangi macho yako, na kujipamba kwa mapambo ya
vito. [41] Huko ulikaa kwenye kitanda kizuri na kwenye meza iliyokuwa imepangwa
mbele yake ulikuwa umeweka ubani na mafuta yangu. [42] Hivyo sauti za watu
zilikuwa zimemzunguka; pamoja na watu wa kila aina, hata walevi waliletwa kutoka
jangwani, na wakawavalisha vikuku mikononi mwao na mataji mazuri juu ya vichwa
vyao. [43] Kisha nikasema juu yake aliyekuwa ameonywa kwa uzinzi, 'Sasa watazini
pamoja naye, na yeye pamoja nao.' [44] Wakamwingilia na kulala naye kama watu
wamwingiliavyo kahaba. Katika njia hii walilala Ohola na Oholiba, waliokuwa
wanawake wazinzi. [45] Lakini watu wenye haki watapitisha hukumu na kuwaadhibu
kama wazinzi, na watawaadhibu kwa hukumu kwa wale wamwagao damu, kwa
sababu wao ni wazinzi na damu iko mikononi mwao. [46] Hivyo Bwana Yahwe asema
hivi: Nitainua kundi la watu juu yao na kuwatoa kuwa kitisho na kuteka nyara.
[47] Kisha hilo kundi la watu litawapiga kwa mawe na kuwakatilia chini kwa panga zao.
Watawaua wana wao na binti na kuzichoma nyumba zao. [48] Kwa kuwa nitaondoa
tabia ya aibu kutoka kwenye nchi na nidhamu wanawake wote hivyo hawatatenda
kama makahaba. [49] Hivyo wataweka tabia yenu ya aibu juu yenu. Mtachukua hatia
ya dhambi zenu pamoja na sanamu zenu, na kwa njia hii mtajua yakuwa mimi ni
Bwana Yahwe.”

# 24

[1] Neno la Yahwe likanijia katika mwaka wa nane mwezi wa kumi na siku ya kumi
ya mwezi, kusema, [2] “Mwanadamu, andika kwa ajili yako jina la hii siku, siku hii
sahihi mfalme wa Babeli ameizingira Yerusalimu. [3] Basi nena mithali juu ya hii
nyumba ya kuasi, fumbo moja. Waambie, 'Bwana Yahwe asema hivi: weka sufuria
ya kupikia. Iweke na weka maji kwenye hiyo. [4] Vikusanye vipande vya chakula
ndani yake, kila kipande kizuri-paja na bega-na ijaze kwa mifupa bora. [5] Chukua
kundi bora na jaza mifupa chini yake. Ilete kuchemsha na ipike mifupa ndani yake.
[6] Kwa hiyo, Bwana Yahwe asema hivi: Ole kwa mji wa damu. Nitakiongeza chungu
cha mbao. Weka kuni nyingi na washa moto. Pika nyama vizuri na changanya
katika viungo na iacha mifupa iteketee. [7] Kwa kuwa damu iko kati yake. Ameiweka
juu ya jiwe laini; hakuimwaga juu ya nchi kuifunika kwa mavumbi, [8] hivyo inaleta
hasira ya kulipa kisasi. Nimeweka damu yake juu ya jiwe laini ili isifunikwe. [9] Kwa
hiyo, Bwana Yahwe asema hivi: Ole kwa mji wa damu. Nitakiongeza chungu cha
mbao. [10] Weka kuni nyingi na washa moto. Pika nyama vizuri na changanya katika
viungo na acha mifupa iteketee. [11] Kisha weka chungu kitupu juu ya mkaa, ili

kuchemsha na kuchoma shaba yake, hivyo uchafu wake ndani yake itayeyushwa,
kutu yake imekula.' [12] Amechoka kwa sababu ya kazi ya taabu, lakini kutu yake
haitoki kweke kwa moto. [13] Tabia yako ya aibu iko ndani ya uchafu wako, kwa
sababu nimekusafisha, lakini bado hutaweza kuwa msafi. Bado hutakuwa huru
kutoka uchafu wako hadi hasira yako itakapotulia kutoka kwako. [14] Mimi, Yahwe,
nimesema hili, na nitalifanya. Sintotulia wala kupumzika kwa ajili ya hili. Kama
njia zako zilivyokuwa, na kama matendo yako, yatakuhukumu! -hivi ndivyo Bwana
Yahwe asemavyo." [15] Kisha neno la Yahwe likanijia, kusema, [16] "mwanadamu!
Tazama, ninachukua tamaa ya macho yako kutoka kwako pamoja na tauni, lakini
hutaomboleza wala kulia, na machozi yako hayatatoka. [17] Utagugumia bila kusikika.
Usiendeshe mazishi kwa ajili ya aliyekufa. Funga kilemba chako juu yako na vaa
makubazi miguuni pako, lakini usivalishe shela nywele zako au kula mkate wa watu
waombolezao kwa ajili ya kuwapoteza wake zao." [18] Hivyo nimeongea na watu
asubuhi, na mke wangu amekufa asubuhi. Asubuhi nimefanya kile nilichokuwa
nimeambiwa kukifanya. [19] Watu wameniuliza, "Ji! hautatuambia haya mambo
yanamaana gani, mambo ambayo unayoyafanya?" [20] Hivyo nimewaambia, "Neno la
Yahwe likanijia, kusema, [21] 'Waambie nyumba ya Israeli, Bwana Yahwe asema hivi:
Tazama! Nitapanajisi patakatifu pangu-fahari ya nguvu yenu, mahali panapopendeza
macho yenu, na panapotamaniwa na roho zenu, na wana wenu na binti zenu
ambao mliowaacha nyuma wataanguka kwa upanga. [22] Kisha mtafanya hasa kama
nilivyofanya: hutafunika nywele za sehemu ya chini za uso, wala kula mkate wa
watu wanaoomboleza! [23] Badala yake, vilemba vyenu vitakuwa juu ya vichwa, na
makubadhi yenu miguuni mwenu; hutaomboleza wala kulia, kwa kuwa mtayeyuka
katika maovu yenu, na kila mtu atagugumia kwa ya ajili ya ndugu yake. [24] Hivyo
Ezekieli atakuwa ishara kwenu, kama kila kitu ambacho alichokifanya mtafanya
wakati hili litakapokuja. Kisha mtajua yakwamba mimi ni Bwana Yahwe!"' [25] "Lakini
wewe, mwanadamu, siku ambayo nitachukua hekalu lao, ambalo ni furaha yao,
kiburi chao, na kile waonacho na kutamani-na wakati nikiwachukua wana wao na
binti- [26] siku hiyo, mgeni atakuja kwako kukupatia habari! [27] Siku hiyo kinywa chako
kitafunguliwa kwa huyo mgeni na utaongea-hutakuwa bubu tena. Utakuwa ishara
kwao hivyo basi watajua kwamba mimi ni Yahwe.

# 25

[1] Kisha neno la Yahwe likanijia, kusema, [2] "Mwanadamu, weka uso wako juu ya
watu wa Amoni na tabiri juu yao. [3] Waambie watu wa Amoni, 'Sikiliza neno la
Bwana Yahwe. Hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo: Kwa sababu umesema, "Aha!"
juu ya patakatifu pangu wakati palipotiwa unajisi, na juu ya nchi ya Israeli wakati
ilipokuwa ukiwa, na juu ya nyumba ya Yuda wakati walipoenda utumwani, [4] kwa
hiyo, tazama, nitakupatia kwa watu katika mashariki kama milki yao. Watafanya
kambi juu yako na kuweka mahema miongoni mwako. Watakula matunda yako na
watakunywa maziwa yako. [5] Nitamfanya Raba malisho ya ngamia na watu wa Amoni
shamba la mifugo. Kisha utajua yakwamba mimi ni Yahwe. [6] Kwa kuwa Bwana
Yahwe asema hivi: Umepigia makofi mikono yako na kupiga chapa miguu yako, na
kufurahi pamoja na dharau ndani yako dhidi ya nchi ya Israeli. [7] Kwa hiyo, tazama!
Nitanyoosha mkono wangu na kukupatia kama mateka kwa mataifa. Nitakukatilia
mbali kutoka watu na kukuangamiza kutoka miongoni mwa nchi! Nitakuharibu, na
utajua yakwamba mimi ni Yahwe.' [8] Bwana Yahwe asema hivi, 'Kwa sababu Moabu
na Seiri husema "Tazama! Nyumba ya Yuda ni kama kila taifa jingine." [9] Kwa hiyo,
tazama! ntafungua miteremko ya Moabu, kuanzia kwenye miji yake juu ya mpaka-
uzuri wa Beth Yeshimothi, Baal Meoni, na Kiriathaimu- [10] kwa watu wa mashariki

waliokuwa juu ya watu wa Amoni. Nitawapatia kama milki ili kwamba watu wa
Amoni hawatakumbukwa miongoni mwa mataifa. 11 Hivyo nitafanya hukumu juu
ya Moabu, na watajua yakwamba mimi ni Yahwe.' 12 Bwana Yahwe asema hivi,
Edomu amelipiza kisasi juu ya nyumba ya Yuda na amefanya makosa katika kufanya
hivyo. 13 Kwa hiyo, Bwana Yahwe asema hivi: Nitaunyoosha mkono wangu juu
ya Edomu na kumharibu kila mtu na wanyama huko. Nitawaharibu, sehemu ya
ukiwa, kutoka Temani hata Dedani. Wataanguka kwa upanga. 14 Nitaweka kisasi
changu juu ya Edomu kwa mkono wa watu wangu Israeli, na watafanya kwa Edomu
kulingana na hasira yangu na ghadhabu yangu, na wakitajua kisasi changu-hivi
ndivyo Bwana Yahwe asemavyo.' 15 Bwana Yahwe asema hivi, 'Wafilisti wamelipiza
kisasi pamoja na uovu na kutoka ndani yao wamejaribu kuiharibu Yuda tena na tena.
16 Basi hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo: Tazam! Nitanyoosha mkono wangu
dhidi ya Wafilisti, na nitakalia mbali Wakerethi na kuwaharibu mabaki yaliyobaki
karibu na pwani. 17 Kwa kuwa nitalipiza kisasi kikubwa dhidi yao pamoja na
matendo ya ghadhabu kubwa ya adhabu, hivyo watajua yakwamba mimi ni Yahwe,
nitakapolipiza kisasi juu yao.”'

# 26

1 Hivyo ilikuwa katika mwaka wa kumi na moja, siku ya kwanza ya mwezi, lile
neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 “Mwanadamu, kwa sababu Tiro amesema juu
ya Yerusalemuu, 'Aha! Malango ya watu waliovunjika! Amenigeukia; Nitajazwa
kwa sababu ameharibika.' 3 Kwa hiyo Bwana Yahwe asema hivi, 'Tazama! Niko
juu yako, Tiro, na nitayainua mataifa mengi juu yako kama bahari iiunuavyo
mawimbi yake. 4 Wataziharibu kuta za Tiro na kuiangusha chini minara yao.
Nitafagia mavumbi yake mbali na kumfanya kama jiwe tupu. 5 Atakuwa sehemu ya
kuwekea nyavu kati ya bahari, kwa kuwa nimesema hilo-hivi ndivyo Bwana Yahwe
asemavyo-na atakuwa mateka kwa ajili ya mataifa. 6 Binti zake walioko mashambani
watachinjwa kwa panga, na watajua kwamba mimi ni Yahwe.' 7 Kwa kuwa hivi
ndivyo Bwana Yahwe asemavyo: Tazama, kutoka kaskazini namleta Nebukadreza
mfalme wa Babeli, mfalme wa wafalme, dhidi ya Tiro, pamoja na farasi na magari
ya farasi, na pamoja na waendesha farasi na watu wengi. 8 Atawaua binti zako
katika shamba. Ataweka kazi ya boma na kujenga ulaghai dhidi ya kuta zako na
kuziinua ngao dhidi yao. 9 Ataweka vyombo vya kubomolea dhidi ya kuta zako,
na vyombo vyake vitaanguka chini ya minara yako. 10 Farasi zake zitakuwa nyingi
kwamba mavumbi yao yatawafunika. Kuta zako zitatikisika kwa mlio wa waendesha
farasi, magurudumu, na magari ya farasi. Wakati atakapoingia malango yako,
ataingia kama watu waingiavyo kwenye mji ambao kuta zimebomolewa. 11 Kwato
za farasi zake zitaikanyaga mitaa yako yote. Atawaua watu wako kwa upanga na
nguzo za uweza wako zitaanguka chini. 12 Watauteka nyara utajiri wako na bidhaa
iliyoporwa. Watabomoa kuta zako na kuziharibu nyumba zako za kifahari. Mawe
yako, mbao zako, na kokoto watazitupa kwenye maji. 13 Nitaikomesha sauti ya
nyimbo zako. Sauti ya vinubi haitasikika tena. 14 Nitakufanya jiwe tupu, utakuwa
mahali ambapo nyavu zitasambazwa kuzikausha. Hutajengwa tena, kwa kuwa mimi,
Bwana Yahwe nimesema-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. 15 Bwana Yahwe
amwambia hivi Tiro, 'Je visiwa havitatetemeka kwa mlio wa kuanguka kwako, na
pamoja na watakaogumia kwa jeraha wakati machinjio mabaya yatakapokuwa kati
yako? 16 Kisha wakuu wote wa bahari watakaposhuka kutoka kwenye viti vyao
vya enzi na kuvua mavazi yao rasmi na kutupa mavazi yaliyonakshiwa. Watavaa
wenyewe kwa kutetemeka, wataketi chini na kutetemeka kila wakati, na wataogopa
kwa sababu yako. 17 Watainua maombolezo juu yako na kukwambia, umekuwaje,

uliyekuwa umekaliwa na manahodha wa meli, umeharibika. Mji mashuhuri ulikuwa
imara sana-sasa umetoka kwenye bahari. Wale wanaoishi ndani yake wanaotia hofu
kuhusu wenyewe juu ya kila mmoja aliyeishi karibu nao. 18 Sasa fukwe zitatetemeka
katika siku ya kuanguka kwako. Visiwa katika bahari vimeogofya, kwa sababu
umekufa.' 19 Kwa kuwa Bwana Yahwe asema hivi: wakati nitakapokufanya wewe
mji kuwa ukiwa, kama miji mingine ambayo haikaliwi, wakati nitakapoviinua vilindi
dhidi yako, na wakati maji makuu yatakapokufunika, 20 kisha nitakushusha chini
kwenda kwa watu wa nyakati za zamani, kama wengingine walioenda chini kwenye
shimo; kwa kuwa nitakufanya uishi katika falme za chini za dunia kama uharibifu
wa nyakati za zamani. Kwa sababu hii hutarudi na kusimama katika nchi ya walio
hai. 21 Nitaweka janga juu yako, na hutakuwepo tena milele. Kisha utatafutwa, lakini
hutapatikana milele tena-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo."

# 27

1 Tena neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 "Sasa wewe, mwanadamu, anza
kuomboleza kuhusiana na Tiro, 3 na mwambie Tiro, aishiye kwenye malango ya
bahari, manahodha wa watu hata visiwa vingi, Bwana Yahwe asema hivi kwako:
Tiro, umesema, mimi ni ukamilifu katika uzuri.' 4 Mipaka yako iko kwenye moyo wa
bahari; majengo yako yamekamilisha uzuri wako. 5 Wametengeneza mbao nene na
pana kwa mvinje kutoka Mlima Hermoni; wamechukua mkangazi kutoka Lebanoni
kuufanya mlingoti. 6 Wametengeneza makasia yako kutoka kwenye mialo ya Bashani;
wametengeza sitaha zako kwa mbao za mvinje kutoka Kitimu, na wametengeneza
kwa pembe. 7 Tanga zako zilikuwa za rangi za kitani kutoka Misri ambazo zilikuwa
kama beramu! 8 Wale waliokuwa wakiishi Sidoni na Arvadi walikuwa wavuta
makasia wako; wenye busara wa Tire walikuwa ndani yenu; walikuwa marubani
wako. 9 Mafundistadi wenye uzoefu wa hali ya juu kutoka Gabeli walijaza mishono;
meli zote za bahari na mabaharia wao miongoni mwenu walikuwa wakiwabeba
manahodha kwaajili ya biashara. 10 Uajemi, Ludi, na Putu walikuwa katika jeshi
lako, watu wako wa vita. Walining'iniza ngao na chapeo ndani yako; walionyesha
uzuri wako. 11 Watu wa Arvadi na Heleki katika jeshi lako walikuwa juu ya kuta zako
wamekuzunguka, na watu wa Gamadi walikuwa kwenye minara yako. Walinin'giniza
juu ngao zao juu ya kuta zako zote zilizokuzunguka! Wakaukamilisha uzuri wako.
12 Tarshishi alikuwa mdau wa biashara pamoja nawe kwa sababu ya wingi wa utajiri
wako wa kuuza mizigo: fedha, chuma, bati, na risasi. Walinunua na kuuza bidhaa
za biashara! 13 Yavani, Tubali, na Mesheki-waliwauza watumwa na katika vitu
kutengeneza shaba. Walibeba bidhaa zako. 14 Beth Togarma waliandaa farasi, farasi
dume, na nyumbu kama kama bidhaa zako. 15 Watu wa Dedani walikuwa wafanya
biashara wako kwenye pwani nyingi. Bidhaa zilikuwa mkononi mwako; walikutumia
pembe, pembe za ndovu, na mpingo kama ushuru! 16 Shamu alikuwa mchuuzi katika
bidhaa zako nyingi; waliandaa zumaridi, zambarau, nguo zenye rangi mbali mbali,
kitambaa kizuri, lulu, na kito chekundu cha thamani kama bidhaa zako. 17 Yuda na
nchi ya Israeli walikuwa wafanyabiashara pamoja nawe. Waliandaa ngano kutoka
Minithi, keki, asali, mafuta, na lihamu kama bidhaa zako. 18 Dameski alikuwa mfanya
biashara wa bidhaa zako zote, za utajiri mkubwa mno, na ya divai ya Helboni na
sufu ya Zahari. 19 Dani na Yavani kutoka Uzali walikwandalia bidhaa ya chuma
kilichofuliwa, na mdalasini, na mchai. Hivi vikawa bidhaa yako. 20 Dedani alikuwa
mchuuzi katika nguo nzuri za kutandika. 21 Arabuni na wakuu wote wa Kedari
walikuwa wafanyabiashara pamoja nawe; walikuandalia wanakondoo, kondoo dume
na mbuzi. 22 Wafanya biashara wa Sheba na Raama walikuja kukuuzia kila aina ya
viungo vizuri katika vito vyote vya thamani; waliuza dhahabu kwa ajili ya bidhaa.

23 Harani, Kane, na Adina walikuwa wafanya biashara pamoja nawe, karibu na Sheba,
Ashuru, na Kilmadi. 24 Hawa walikuwa wachuuzi wako mapambo ya joho ya nguo za
urujuani pamoja na rangi zilibuniwa, na nguo zilizo sanifiwa vizuri katika sehemu
zako za soko. 25 Merikebu za Tarshishi zilikuwa misafara ya bidhaa yako! Hivyo
ulijaa, shehena nzito katika moyo wa bahari! 26 Wapiga makasia wako walikuleta
kwenye bahari kuu mno; upepo wa mashariki umekuvunja kati yao. 27 Utajiri wako,
bidhaa, na mizigo ya biashara; wapiga makasia wako na marubani, na waunzi wa
meli; wafanya biashara wako wa bidhaa na watu wote wa vita walio ndani yako,
na jeshi lako-watazama kwenye kina cha bahari siku ya kuangamia kwako. 28 Miji
iliyopo kwenye bahari sauti itatetemeka kulia kwa rubani zako; 29 Wote wavutao
kasia watashuka chini kutoka meli katika zao; wanamaji na marubani wote juu
ya bahari watasimama juu ya nchi. 30 Kisha watakufanya kusikiliza sauti yao na
kulia kwa uchungu; watarusha vumbi juu ya vichwa vyao. Watabingirika katika
majivu. 31 Watanyo vichwa vyao upara kwa ajili yako na kujifunga wenyewe kwa
nguo za magunia, na watalia kwa sauti. 32 Watakuinulia maombolezo ya kuomboleza
kwa ajili yako na kuimba nyimbo za maombolezo juu yako, ni nani aliye kama
Tiro, ambaye sasa ameletwa kunyamazishwa kati ya bahari? 33 Wakati bidhaa yako
ilipoenda ufukweni kutoka kwenye bahari, imewarithisha watu wengi; uliwatajirisha
wafalme wa dunia kwa wingi wa utajiri wako mkubwa na bidhaa! 34 Lakini wakati
ulipo vunjwavunjwa kwa bahari, kwa vilindi vya maji, bidhaa yako na wafanya kazi
wako wote kuzama! 35 Wote wakaao pwani walikuogopa, na wafalme wao kuvunjwa
vunjwa katika kitisho! Nyuso zao zimetetemeka! 36 Wafanya biashara wa meli wa
watu wakuzomea; umekuwa tishio, na hutakuwepo tena milele."

# 28

1 Kisha neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 "Mwanadamu, waambie watawala wa
Tiro, 'Bwana Yahwe asema hivi: Moyo wako unakiburi! Umesema, "mimi ni mungu!
Nitakaa kwenye kiti cha miungu katika moyo wa bahari!" Ingawa wewe ni mtu
na sio mungu, unaufanya moyo wako kama moyo wa mungu, 3 unafikiri kwamba
unahekima kuliko Danieli, na kwamba hakuna siri ikushangazayo! 4 Umejitajirisha
mwenyewe pamoja na hekima na ujuzi, na kujipatia dhahabu na fedha katika hazina
yako! 5 Kwa hekima kubwa na kwa biashara yako, umeongeza utajiri wako, hivyo
moyo wako una kiburi kwa sababu ya utajiri yako. 6 Kwa hiyo, Bwana Yahwe
asema hivi: Kwa sababu umetengeza moyo wako kama moyo wa mungu, 7 kwa
hiyo nitaleta wageni juu yako, watu wa kuogofya kutoka mataifa mengine. Wataleta
panga zao juu hekima ya uzuri wako, na watauchafua uzuri wako. 8 Watakupeleka
chini hata kwenye shimo, na utakufa kifo cha waliokufa katika Bahari. 9 Je! kweli
utasema, "Mimi ni mungu" mbele ya uso wa yule akuuaye? Wewe ni mwanadamu
na sio Mungu, na utakuwa kwenye mkono wa yule akujeruaye. 10 Utakufa kifo cha
asiyetahiriwa kwa mkono wa wageni kwa kuwa nimesema hili-asema Bwana Yahwe.
11 Neno la Yahwe likanijia, kusema, 12 "Mwanadamu, inua maombolezo kwa ajili
ya mfalme wa Tiro na umwambie, 'Bwana Yahwe asema hivi: Uliumbwa mkamilifu,
umejaa hekima na ukamilifu wa hekima. 13 Ulikuwa katika Edeni, bustani ya Mungu.
Kila jiwe la thamani lilikufunika: akiki, yakuti manjano, almasi, zabarajadi, shohamu,
yaspi, yakuti samawi, zumaridi, baharamani, na dhahabu. Ilikuwa siku uliyokuwa
umeiumba ambayo walikuwa wameiandaa. 14 Nimekuweka juu ya mlima mtakatifu
wa Mungu kama kerubi nimekutia mafuta kwa ajili ya kumlinda mwanadamu.
Ulikuwa kati ya mawe ya moto ulipozunguka. 15 Ulikuwa mwadilifu kwenye njia
zako kutoka siku ulipoumbwa hadi uovu ulipoonekana ndani yako. 16 Kupitia
biashara yako kubwa uliyokuwa umeijaza kwa udhalimu, hivyo umetenda dhambi.

Hivyo nimekutupilia mbali ya mlima wa Mungu, kama mmoja wao wa aliyekuwa
ameninajisi, na nimekuharibu, kerubi mlinzi, na kukutoa miongono mwa mawe
ya moto. 17 Moyo wako ulikuwa na kiburi kwa uzuri wako; umeiharibu hekima
yako kwa sababu ya fahari yako. Nimekupeleka chini kwenye dunia. Nimekuweka
mbele ya wafalme ili waweze kukuona. 18 Kwa sababu ya wingi wa dhambi zako na
biashara za udanganyifu, umepanajisi mahali pako patakatifu. Basi nimetengeneza
moto kutoka ndani yako; utakula wewe. Nitakugeuza kwenye majivu juu ya dunia
katika macho ya wote wakutazamao. 19 Wale wote waliokujua miongoni mwa watu
watakao kutetemekewa; watakuwa watu wa kutisha, na hutakuwepo tena milele.”'
20 Kisha neno la Bwana Yahwe likanijia, kusema, 21 “Mwanadamu, elekeza uso wako
Sidoni na toa utabiri juu yake. 22 Sema, Bwana Yahwe asema hivi: Tazama! Niko
juu yako, Sidoni! Kwa kuwa nitatukuzwa kati yako hivyo watu wako watajua
kwamba mimi ni Yahwe wakati nitakapokuwa nimezitekeleza hukumu ndani yako.
Nitaonyesha utakatifu ndani yako. 23 Nitapeleka tauni juu yako na tazama mitaa
yako, na walioua wataanguka kati yako. Wakati upanga utakapokuja juu yao kutoka
pande zote, kisha mtajua kwamba mimi ni Yahwe. 24 Kisha hakutakuwa na mtemba
uchomao na maumivu ya miba kwa ajili ya nyumba ya Israeli kutoka wale wote
waliomzunguka wanaowadharau watu wake, hivyo watajua kwamba mimi ni Bwana
Yahwe!' 25 Bwana Yahwe asema hivi, Nitakapowakusanya nyumba ya Israeli kutoka
miongni mwa watu waliokuwa wamekusanyika, na wakati nilipokuwa nimewatenga
miongoni mwao, hivyo mataifa aanaweza kuona, kisha watafanya nyumba zao katika
nchi nitakayo mpatia mtumishi wangu Yakobo. 26 Kisha wataishi salama ndani yake
na kujenga nyumba, kulima mizabibu, na kuishi salama wakati nitakapo zitekeleza
hukumu juu ya wote wale ambao sasa wanawadharau kutoka sehemu zote; basi
watajua yakwamba mimi ni Yahwe Mungu wao!”'

# 29

1 Katika siku ya kumi, katika mwezi wa kumi siku ya kumi na moja ya mwezi,
neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 “Mwanadamu, weka uso wako juu ya Farao,
mfalme wa Misri; toa unabii juu yake na juu ya Israeli yote. 3 Nena na sema, 'Bwana
Yahwe asema hivi: Tazama! Ni juu yako, Farao, mfalme wa Misri. Wewe joka
kubwa ambaye ujifichaye kati ya mto, husema, “Mto wangu ni wangu mwenyewe.
Nimeufanya kwa ajili yangu mwenyewe.” 4 Kwa kuwa nitaweka kalabu katika taya
zako, nasamaki za mto wako zitashikamana na magamba yako; nitakuinua juu kutoka
kati ya mto wako karibu na samaki zote za mto walioshikamana na maganda yako.
5 Nitakutupa chini kwenye jangwa, wewe pamoja na samaki wako wote kutoka
kwenye mto wako. Utaanguka kwenye shamba la wazi; hutakusanya wala kuinua.
Nitakupatia kama chakula kwa viumbe hai vya dunia na kwenye ndege wa angani.
6 Kisha wote wakaao Misri watajua kwamba mimi Yahwe, kwa sababu wamekuwa
mwanzi wa kutegemewa hata kwenye nyumba ya Israeli. 7 Wakati watakapokushika
kwa mkono wao, ulivunjika na kurarua wazi mabega yao; na watakapojifunza juu
yako, ulivunjika, na kusababisha miguu yao kutokuwa imara. 8 Kwa hiyo Bwana
Yahwe asema hivi: Tazama! nitaleta upanga juu yako. Nitawakatilia mbali wote
mwanadamu na mnyama mbali nawe. 9 Hivyo nchi ya Misri itakuwa ukiwa na
jangwa. Ndipo watakapojua kwamba mimi ni Yahwe, kwa sababu jitu la kutisha
liliseama, “Huu mto ni wangu, kwa kuwa nimeufanya mimi.” 10 Kwa hiyo, tazama!
Ni juu yako na juu ya mto wako, hivyo nitaitoa nchi ya Misri juu ya ukiwa na
jangwa, na utakuwa nchi yenye jangwa kutoka Migdoli hata Sewene na mipaka ya
Kushi. 11 Hakutakuwa na mguu wa mtu kupitia, na hakuna mguu wa wanyama pori
watakao upitia. Haitakuwa makao kwa miaka arobaini. 12 Kwa kuwa nitaifanya nchi

ya Misri kuwa ukiwa kati ya nchi zilizoharibiwa, na miji yake kati ya miji isiyotumika
itakuwa ukiwa kwa miaka arobaini; kisha nitaitawanya Misri miongoni mwa mataifa,
nitawatapanya kati ya nchi mbali mbali. 13 Kwa kuwa Bwana Yahwe asema hivi:
Mwisho wa miaka arobaini nitaikusanya Misri kutoka kwa watu miongoni mwao
wale waliokuwa wametawanyika. 14 Nitawarudisha wageni wa Misri na kuwarudisha
hata mkoa wa Pathrosi, hata kwenye nchi ya asili yao. Kisha huko watakuwa
ufalme wa chini. 15 Utakuwa chini ya falme, na hautajiinua tena juu ya mataifa.
Nitawapunguza hivyo hawatatawala tena juu ya mataifa. 16 Wamisri hawatakuwa
sababu kwa ajili ya imani kwa ajili ya nyumba ya Israeli. Badala yake, watakuwa
kumbusho la uovu ambao Israeli umeufanya walipogeukia Misri kwa ajili ya msaada.
Kisha watajua kwamba mimi ni Bwana Yahwe.”' 17 Kisha ikawa katika mwaka wa
ishirini na saba siku ya kwanza ya mwezi, lile neno la Yahwe likanijia, kusema,
18 “Mwanadamu, Nebukadreza mfalme wa Babeli amelinda jeshi lake kufanya kazi
ngumu juu ya Tiro. Kila kichwa kilitiwa upara, na kila bega lilifanywa mali ghafi.
Kisha yeye na jeshi lake hawakupokea malipo kutoka Tiro kwa kazi ngumu aliyokuwa
ameimaliza dhidi yake. 19 Kwa hiyo Bwana Mungu asema hivi, 'Tazama! ninawapatia
Nebukadreza nchi ya Misri mfalme wa Babeli, na atachukua utajiri wake, kuziteka
nyara milki zake, na kuchukua yote atakayoyakuta huko; nayo yatakuwa mshahara
wa jeshi lake. 20 Nimempatia nchi ya Misri kama mshahara kwa ajili ya kazi
waliyonifanyia-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. 21 siku hiyo nitachipusha pembe
kwa ajili ya nyumba ya Israeli, na nitakufanya uzungumze kati yao, ili kwamba wajue
yakwamba mimi ni Yahwe.”'

# 30

1 Neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 “Mwanadamu, toa unabii na sema, 'Bwana
Yahwe asema hivi: Maombolezo. “Ole unakuja siku hiyo.” 3 siku ikaribu. Siku
ikaribu kwa ajili ya Yahwe. Itakuwa siku ya mawingu, mda wa hukumu kwa ajili
ya mataifa. 4 Kisha upanga utakuja dhidi ya Misri, na huko kutakuwa na maumivu
makali katika Kushi wakati wauaji wa watu watakapoanguka katika Misri-wakati
watakapochukua utajiri, na wakati misingi yake itakapoharibiwa. 5 Kushi, Putu,
na Ludi, na wageni wote, pamoja na watu wa nyumba ya agano-wote wataanguka
chini kwa upanga. 6 Yahwe asema hivi: Basi wale wanaoisaidia Misri wataanguka,
na kiburi cha uweza wake kitashuka chini. Kutoka Migdoli hata Sewene maaskari
wao wataanguka kwa upanga-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. 7 Wataogofya
kati ya nchi zilizotupwa, na miji yao itakuwa miongoni mwa miji yote iliharibika.
8 Kisha watajua kwamba mimi ni Yahwe, nitakapouweka moto katika Misri, na wakati
wasaidizi wake wote watakapoharibiwa. 9 Katika siku hiyo wajumbe watatoka mbele
yangu katika meli ili kuitia hofu Kushi iliyo salama, na kutakuwa na maumivu makali
miongoni mwao katika siku ya kuangamizwa Misri. Kwa kuwa tazama! inakuja.
10 Bwana Yahwe asema hivi: Nitaufanya mwisho wa watu wa Misri kwa mkono
wa Nebukadreza, mfalme wa Babeli. 11 Yeye na jeshi lake pamoja naye, hofu ya
mataifa, italetwa kuiharibu nchi; watafuta panga zao juu ya Misri na kuijaza nchi
pamoja na watu waliokufa. 12 Nitaifanya mito kuwa nchi kavu, na nitaiuza nchi
kwenye mkono wa watu waovu. Nitaifanya nchi na viijazavyo ukiwa kwa mkono
wa wageni-mimi, Yahwe, nimesema. 13 Bwana Yahwe asema hivi: Nitaziharibu
sanamu, na nitaleta mwisho wa sanamu za ubatili za Nofu. Hakutakuwa na mkuu
katika Misri, na nitaweka hofu katika nchi ya Misri. 14 Kisha nitaifanya Pathrosi
ukiwa na kuweka moto katika Soani, nitatekeleza matendo ya hukumu katika No.
15 Kwa kuwa nitamwaga ghadhabu yangu juu Sini, ngome ya Misri, na kuwakatilia
mbali watu wa mataifa. 16 Kisha nitaweka moto katika Misri; Sini itakuwa katika

dhiki kuu, No itavunjika, na Nofu itakabiliana na maadui kila siku. 17 Vijana
katika Oni na Pi-besethi wataanguka kwa upanga, na miji yao itaenda utumwani.
18 Huko Tapanesi, siku itabadilika kuwa usiku nitakapo ivunja nira ya Misri huko,
na kiburi cha uwezo wake kitaisha. Kutakuwa na wingu likimfunika, na binti
zake wataenda utumwani. 19 Nitatekeleza matendo ya hukumu katika Misri, hivyo
watajua kwamba mimi ni Yahwe."' 20 Kisha ikawa katika mwaka wa kumi na
moja, katika mwezi wa kwanza, katika siku ya saba ya mwezi, lile neno la Yahwe
likanijia, kusema, 21 "Mwanadamu, nimeuvunja mkono wa Farao, mfalme wa Misri.
Tazama! Haukufungwa, au kufungwa kwa kitambaa cha bendeji ili upone, hivyo basi
uweze kuwa imara kushika upanga. 22 Kwa hiyo Bwana Yahwe asema hivi, 'Tazama,
mimi niko juu ya Farao, mfalme wa Misri. Kwa kuwa nitauvunja mkono wake,
wote yule aliye hodari na yule aliyevunjika, nitaufanya upanga wangu kuanguka
kutoka kwenye mkono wake. 23 Kisha nitaitawanya Misri miongoni mwa mataifa
na kuwatawanya katika nchi mbali mbali. 24 Nitaunyoosha mikono kwa mfalme wa
Babeli na kuweka upanga wangu katika mkono wake ili kwamba niweze kuiharibu
mikono ya Farao. Atagugumia mbele ya mfalme wa Babeli kwa mgumio wa mtu
anayekufa. 25 Kwa kuwa nitainyoosha mikono ya mfalme wa Babeli, wakati mkono
wa Farao utakapoanguka. Kisha watajua yakwamba mimi ni Yahwe, nitakapoweka
upanga wangu kwenye mkono wa mfalme wa Babeli; kwa kuwa ataishambulia nchi
ya Misri kwa huo. 26 Hivyo nitaitawanya miongoni mwa mataifa na kuyatawanya
kwenye nchi tofauti tofauti. Kisha watajua yakwamba mimi ni Yahwe."'

# 31

1 Kisha ikawa katika mwaka wa kumi na moja, katika mwezi wa tatu, siku ya
kwanza ya mwezi, lile neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 "Mwanadamu, mwambie
Farao, mfalme wa Misri, na watu wake wanaomzunguka, 'Katika ukuu wako, je!
wewe ni kama nani? 3 Tazama! Ashuru ilikuwa mwerezi katika Lebanoni pamoja
na matawi mazuri, yakitoa kivuli kwenye msitu, na mirefu katika kimo, na matawi
yalitengeneza kilele cha mti wake. 4 Maji mengi yaliufanya kuwa mrefu; maji ya
chini yaliufanya kuwa mkuba. Mito ilitiririka sehemu zake zote, kwa kuwa mifereji
yake ilitoa kuelekea kwenye miti yote katika shamba. 5 Kimo chake kikubwa kilikuwa
zaidi kuliko miti mingine yote katika shamba, na matawi yake yakawa mengi; matawi
yake yalikuwa marefu kwa sababu ya maji mengi yalipokuwa yakikua. 6 Kila ndege
wa mbinguni alitengeza kiota kwenye matawi yake, wakati kila kiumbe hai cha
shamba kilizaa mtoto chini ya tawi. Mataifa mengi yote yaliishi chini ya kivuli
chake. 7 Kwa kuwa ulikuwa uzuri katika ukuu wake na kimo cha matawi yake, kwa
kuwa mizizi yake ilikuwa katika maji mengi. 8 Mierezi katika bustani ya Mungu
haikuweza kuwa sawa nayo. Hakuna miongoni mwa miti ya mivinje iliyofanana
matawi yake, na miti ya miamori haikuweza kuwa sawa na majani yake. Hapakuwa
na mti mwingine katika bustani ya Mungu ulikuwa kama huo katika uzuri wake.
9 Nimeufanya kuwa mzuri pamoja na matawi yake mengi na miti yote ya Edeni
iliyokuwa katika bustani ya Mungu ilimwonea wivu. 10 Kwa hiyo Bwana Yahwe
asema hivi: Kwa sababu ilikuwa mirefu kwa kina, na imekiweka kilele chake kati
ya matawi yake, moyo wake umeinua kwa sababu ya urefu wake. 11 Nimeuweka
kwenye mikono ya yeye mwenye uweza wa mataifa, kuishughulikia kulingana na
yale maovu anayostahili. Nimeufukuza. 12 Wageni waliokuwa wakiogofya wa mataifa
yote wameikatilia mbali kuiacha ife. Matawi yake yameanguka kwenye milima na
mabonde yote, na matawi yake yameanguka katika mito yote ya nchi. Kisha mataifa
yote juu ya nchi wakatoka nje kutoka chini ya kivuli na kwenda zao wakamwacha.
13 Ndege wa agani watapumzika kwenye shina la mti ulioanguka, na kila mnyama

wa shambani atakuja kwenye matawi yake. 14 Hii litokea ili kwamba pasiwe na
miti mingine itakayopandwa karibu na maji yatang'oa majani yake hata kwenye
kina cha miti mirefu, na kwamba hakuna miti mingine itakayomea karibu na maji
itakayofikia kwenye hicho kina. Wote wametolewa kufa, chini ya nchi, miongoni
mwa watoto wa binadamu, pamoja na wale washukao chini. 15 Bwana Yahwe asema
hivi: Katika siku wakati mkangazi uliposhuka chini nilileta maombolezo kwenye
dunia. Niliyafunika maji ya chini juu yake, nikayarudisha maji ya bahari. Nilizuia
maji makuu, nikaleta maombolezo hata Lebanoni kwa ajili yake. Hivyo miti yote
ya shambani ikaomboleza kwa sababu yake. 16 Nimeleta tetemeko kwa mataifa wa
sauti ya kuanguka kwake, wakati nitakapomtupa chini mpaka kuzimu pamoja na
wale walioenda chini kwenye shimo. Hivyo niliitia moyo miti ya Edeni yote katika
pande zote za nchi. Hii ilikuwa imechaguliwa na miti iliyokuwa bora ya Lenanoni;
miti iliyokunywa maji. 17 Kwa kuwa walikwenda chini pia pamoja nayo hata kuzimu,
kwa wale waliokuwa wameuawa kwa upanga. Kulikuwa na jeshi lake imara, yale
mataifa yalikuwa yakiishi kati kivuli chake. 18 Umefanana na nani hivi katika utukufu
na ukuu kati ya mti wa Edeni? Kwa kuwa utashushwa chini pamoja na miti ya Edeni
hata pande zote nne za dunia miongoni mwa wasiotahiriwa; utaishi pamoja na watu
wake wote-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavy."

# 32

1 Kisha ikawa katika mwezi wa kumi na mbili wa mwaka wa kumi na mbili,
siku ya kwanza ya mwezi, lile neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 "Mwanadamu,
inua maombolezo kuhusu Farao mfalme wa Misri; mwambie, 'Wewe ni kama
simba mdogo juu ya mataifa, lakini kama jitu la kutisha, unatoka kwenye maji,
unayachafua maji kwa miguu yako na kuyachafua maji yao. 3 Bwana Yahwe asema
hivi: Basi nitautandaza wavu wangu juu yako katika kusanyiko la watu wengi, na
watawainua juu katika wavu wangu. 4 Nitakuacha katika nchi. Nitakutupa kwenye
shamba na kufanya ndege wote wa angani watue juu yako; njaa ya wanyama
wote waishio juu ya nchi watashibishwa na wewe. 5 Kwa kuwa nitaiweka nyama
yako juu ya milima, na nitayajaza mabonde kwa funza wako waliokufa. 6 Kisha
nitamwaga damu yako juu ya milima, na vitanda vya kijito vitajazwa kwa damu
yako. 7 Kisha wakati nitakapokuzimisha, nitazifunika mbingu na kuzitia giza nyota
zake; nitalifunika jua kwa mawingu, na mwezi hautatoa nuru yake usiku. 8 Mianga
ya mbinguni nitaiweka giza juu yako, na nitaweka giza juu ya nchi-hivi ndivyo
asemavyo Bwana Yahwe. 9 Hivyo nitaitisha mioyo ya watu wengi katika nchi ambao
huwajui, wakati nitakapoleta kuhusu uvunjifu miongoni mwa mataifa, miongoni
mwa nchi ambazo hukuzijua. 10 Nitawashangaza watu wengi kuhusiana na wewe;
wafalme wao watatetemeka kwa hofu kuhusiana na wewe nitakapoutikisa upanga
wangu mbele yao. Kila wakati kila mmoja atatetemeka kwa sababu yako, katika
siku ya kuanguka kwako. 11 Kwa kuwa Bwana Yahwe asema hivi: Upanga wa
mfalme wa Babeli utakuja juu yako. 12 Nitawafanya watu wako kuanguka kwa panga
za mashujaa-kila shujaa ni tishio la mataifa. Hawa mashujaa watateketeza kiburi
cha Misri na kuangamiza watu wake wote. 13 Kwa kuwa nitaiharibu mifugo yote
kutoka karibu na maji mengi; na mguu wa mtu hautayatibua tena, wala kwato za
wanyama hazitayatibua. 14 Kisha nitayafanya maji yao kuwa matulivu na kufanya
mito yao kukimbia kama mafuta-hivi ndivyo asemavyo Bwana Yahwe. 15 Wakati
nitakapoifanya nchi ya Misri sehemu iliyojitenga, wakati nchi iliyopungukiwa na vitu
viijazavyo, wakati nitakapo washambulia wakaao ndani yake, watajua yakwamba
mimi ni Yahwe. 16 Kutakuwa na maombolezo; binti za mataifa wataomboleza juu
yake; wataomboleza juu ya Misri, juu ya watu wake wote wataomboleza-hivi ndivyo

Bwana Yahwe asemavyo.”' 17 Kisha ikawa katika mwaka wa kumi na mbili, siku
ya kumi na tano ya mwezi, lile neno la Yahwe likanijia, kusema, 18 “Mwanadamu,
omboleza kwa ajili watu wa misri na walete chini-yeye na binti za mataifa mashuhuri-
hata chini ya dunia pamoja na wale walioshuka chini kwenye shimo. 19 'Je! wewe
ni mzuri zaidi kuliko mtu mwingine yeyote? Nenda chini na lala chini pamoja
na wasiotahiriwa.' 20 Wataanguka miongoni mwao waliokuwa wameuawa kwa
upanga. Upanga ulikuwa umewekwa! Alikuwa amepatiwa upanga; watamkamata
na watu wake. 21 Hodari wa wapiganaji katika Sheoli atasema kuhusu Misri na
rafiki zake, 'Wameshuka chini hapa! Watalala pamoja na wasiotahiriwa, pamoja
na wale waliokuwa wameuawa kwa upanga.' 22 Ashuru yupo huko pamoja na
kusanyiko lake. Makaburi yake yamemzunguka; wote waliuawa kwa upanga. 23 Wale
ambao makaburi yao yamewekwa katika maficho ya mashimo yaliyo huko, pamoja
na kusanyiko lake. Makaburi yake yakiwazunguka wote waliokuwa wameuawa,
walioanguka kwa upanga, wale walioleta hofu juu ya nchi ya walio hai. 24 Elamu
yupo huko pamoja na watu wake wote. Makaburi yake yamemzunguka; wote
walikuwa wameuawa. Wale walioawa kwa upanga, walioshuka chini wasiotahiriwa
hata sehemu ya chini kabisa ya dunia, waliowatia hofu juu ya nchi ya walio hai
na wale waliobeba aibu yao wenyewe, pamoja na wale washukao chini kwenye
shimo. 25 Wamemuwekea kitanda kwa ajili ya Elamu na watu wake wote kati ya
wachinjaji; kaburi lake limemzunguka. Wote hawajatahiriwa, kukatwa vipande kwa
upanga, kwa sababu waliwaleta mashujaa wao juu ya nchi ya walio hai. Hivyo
wamechukua aibu yao wenyewe, pamoja na wale washukao kwenye shimo miongoni
mwa wote waliouawa, wale washukao kwenda shimoni. Elamu yu miongoni mwa
wale waliokuwa wameuawa. 26 Mesheki, Tubali, na watu wake wote wako huko!
Makaburi yao yamewazunguka. Wote hawajatahiriwa, wameuawa kwa upanga, kwa
sababu walileta utiisho wao juu ya nchi ya walio hai. 27 Wasilale pamoja mashujaa
walioanguka wa wasiotahiriwa walioshuka chini kwa Sheoli pamoja na silaha zao
zote za vita, na pamoja na panga zao zote walizoziweka chini ya vichwa vyao na
maovu yao juu ya mifupa yao. Kwa kuwa walikuwa tishio kwa mashujaa katika
nchi ya walio hai. 28 Basi wewe, Misri, utavunjika kati yao wasiotahiriwa! Utalala
karibu nao waliokuwa wamekatwa vipande vipande kwa upanga. 29 Edomu yuko
huko na wafalme na viongozi wake wote. Walikuwa wamehifadhiwa katika uwezo
wao pamoja na wale walioawa kwa upanga. Pamoja na wasiotahiriwa wamelala,
pamoja na wale walioshuka kwenye shimo. 30 Wakuu wa kaskazini wako huko-
wote na Wasidoni wote walioshuka chini pamoja na hao waliokuwa wamekatwa
vipande vipande. Walikuwa na nguvu na kuwafanya wengine kuogopa, lakini sasa
wako huko kwa aibu, wasiotahiriwa pamoja na wale waliokatwa vipande vipande
kwa upanga. Wamebeba aibu yao wenyewe, pamoja nao waendao kwenye shimo.
31 Farao ataona na kupata faraja kuhusu kundi lake waliokatwa vipande vipande kwa
upanga -Farao na jeshi lake lote-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. 32 Natamuweka
kama utiisho wangu katika nchi ya walio hai, lakini atakuwa amelazwa chini katikati
yao wasiotahiriwa, miongoni mwa wale walio katwa vipande kwa upanga, Farao na
makundi yake yote-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo.

# 33

1 Kisha neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 “Mwanadamu, sema hivi kwa watu wako;
waambie, 'Nitakapoleta upanga juu ya nchi, kisha watu wa hiyo nchi wakamchukua
mtu mmoja kutoka mingoni mwao na kumfanya awe mlinzi wao. 3 Atazamapo kwa
upanga kama unakuja juu ya nchi, na apige tarumbeta kuwaonya watu! 4 Kama watu
wakisikia sauti ya tarumbeta lakini bila kusikia, na kama upanga ukija na kuwaua,

kisha damu ya kila mmoja iko juu ya kichwa chake mwenyewe. [5] Kama mtu akisikia
sauti ya tarumbeta na hakusikiliza, damu yake iko juu yake; lakini kama akisikia,
ataokoa maisha yake mwenyewe. [6] Bali, kama mlinzi akiona upanga unakuja, lakini
kama asipopiga tarumbeta, pamoja na matokeo kwamba watu hawajaonywa, na
kama upanga ukija na kuchukua uhai wa mtu yeyote, kisha yule mtu akafa kwenye
dhambi yake mwenyewe, lakini nitaitaka damu yake kutoka mlinzi.' [7] Sasa wewe
mwenyewe, mwanadamu! Nimekufanya kuwa mlinzi kwa ajili ya nyumba ya Israeli;
utasikia maneno kutoka kinywani mwangu na uwaonye badala yangu. [8] Kama
nikimwambia mtu mwovu, 'Mwovu, hakika utakufa!' lakini kama hutangazi hivi
ili kwa ajili ya kumuonya mtu mwovu kuhusu hii njia, kisha huyo mtu mwovu
atakufa katika dhambi yake, lakini nitaitaka damu yake kutoka kwenye mkono
wako! [9] Lakini wewe, kama ukimwonya mwovu kuhusu hii njia, hivyo basi anaweza
kurudi kutoka hiyo, na kama kama asipogeuka kutoka njia yake, kisha atakufa katika
dhambi yake, lakini wewe mwenyewe utakuwa umeokoa maisha yako. [10] Basi wewe,
mwanadamu, sema kwa nyumba ya Israeli, 'Mnasema hivi, Makosa yetu na dhambi
zetu zi juu yetu, na tunadhoofika kwa ajili yao! Je! tutaishije?"' [11] Waambie, 'Kama
niishivyo-asema Bwana Yahwe-sifurahii kifo cha mwovu, kwa kuwa kama mwovu
akitubu kutoka njia yake, kisha ataishi! Tubu! Tubu kutoka njia zako mbaya!
Kwa nini mnataka kufa, nyumba ya Israeli?' [12] Hivyo basi wewe, mwanadamu,
waambe watu wako, 'Haki ya mwenye haki haitamwokoa kama akikosa! Uovu wa
mtu mwovu hautamfanya kuangamia kama akitubu dhambi zake! Kwa kuwa mtu
mwenye haki hataweza kuishi kwa sababu ya haki yake kama akikosa. [13] Kama
nikisema kwa mwenye haki, "Hakika ataisha!" na kama akiamini katika haki yake
na kisha akafanya udhalimu, sitokumbuka haki yake yoyote. Atakufa kwa ajili ya
uovu alioufanya. [14] Hivyo kama nikisema kwa mwovu, "Utakufa hakika," lakini
kama akitubu kutoka kwenye dhambi zake na kufanya yaliyo halali na haki- [15] kama
akirudisha dhamana ambayo aliyomnyang'anya, au kama akirudisha alichokipoteza,
na kama akitembea katika amri zitoazo uhai na bila kufanya dhambi-kisha ataishi
hakika. Hatakufa. [16] Dhambi alizozifanya hazitakumbukwa kwa ajili yake. Ametenda
halali na haki, na hivyo, ataishi hakika! [17] Lakini watu wako husema, "Njia ya
Bwana haiko sawa!" lakini ni njia zako ndizo haziko sawa! [18] Wakati mtu mwenye
haki ageukapo kutoka kwenye haki na kufanya dhambi, kisha atakufa katika hiyo!
[19] Wakati mtu mbaya ageukapo kutoka kwenye ubaya wake na kufanya iliyo halali
na haki, ataishi kwa sababu ya hayo mambo! [20] Lakini ninyi watu husema, "Njia
ya Bwana haiko sawa!" Nitawahukumu kila mmoja wenu kulingana na njia yake,
nyumba ya Israeli!"' [21] Ikawa katika mwaka wa kumi na mbili, siku ya tano ya
mwezi wa kumi ya uhamisho wetu, mtu mmoja akatoroka kutoka Yerusalemuna
kusema, "Mji umetekwa!" [22] Mkono wa Yahwe ulikuwa juu yangu jioni kabla yule
mtoro hajaja, na mdomo wangu ulikuwa wazi mda huo alikuja kwangu wakati wa
mapambazuko. Hivyo mdomo wangu ulikuwa wazi; sikuwa bubu tena! [23] Kisha neno
la Yahwe likanijia, kusema, [24] "Mwanadamu, wale waishio mahali palipoharibika
katika nchi ya Israeli huongea na kusema, 'Ibrahimu alikuwa mtu pekee, na alirithi
nchi, lakini sisi tukowengi! Tumepewa nchi kama wamiliki." [25] Kwa hiyo waambie,
'Bwana Yahwe asema hivi: Mnakula damu, na mmeziinulia macho yenu sanamu,
kisha mnazimwagia damu za watu. Je! mna uhakika wa kuimiliki hii nchi?
[26] Mnategemea upanga wenu na mmetenda mambo maovu; kila mtu amemnajisi
mke wa jirani yake. Je! kweli mtaimiliki nchi?' [27] Utawaambia hivi, 'Bwana Yahwe
asema hivi: Kama niishivyo, hakika wale walio katika uharibifu wataanguka kwa
upanga, na nitawapatia wale walio katika mashamba viumbe hai kama chakula, na
wale walio katika ngome na mapango watakufa kwa tauni. [28] Kisha nitairudisha

nchi kwenye ukiwa na tishio, na kiburi cha uwezo wake kitakoma, kwa kuwa milima
ya Israeli itakuwa jangwa, na hakutakuwa na mtu yeyote atakayewapitia.' 29 Hivyo
watajua kwamba mimi ni Yahwe, nitakapoifanya nchi ukiwa na tishio kwa sababu
ya machukizo yote waliyoyafanya. 30 Hivyo basi wewe, mwanadamu-watu wako
wanasema mambo yako karibu na kuta na malango ya nyumba, na kila mmoja
anaambizana na mwenzake-kila mtu na ndugu yake, 'Twende na tukasikilize neno la
nabii lililotoka kwa Yahwe! 31 Hivyo watu wangu watakuja kwako, kama wafanyavyo
mara nyingi, na nitaketi mbele yako na kusikiliza maneno yako, lakini mioyo yao
inafuata udhalimu kwa faida yao. 32 Kwa kuwa umekuwa kama wimbo mzuri kwao,
sauti nzuri awezaye kucheza kinanda vizuri, hivyo watasikia maneno yako, lakini
hakuna atakaye yatii. 33 Hivyo wakati haya yote yatakapotokea-tazama! itatokea!
-watajua yakwamba nabii alikuwa miongoni mwao."

# 34

1 Kisha neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 "Mwanadamu, tabiri dhidi ya wachungaji
wa Israeli. Toa unabii na waambie, 'Bwana Yahwe asema hivi kwa wachungaji:
Ole kwa wachungaji wa Israeli wanaojilisha wenyewe. Je! wachungaji hawapaswi
kulilinda kundi? 3 Mnakula mafungu yaliyonona na mnavaa sufu. Mnawachinja
walionona. Hamkuwalisha siku zote. 4 Hamkuwatia nguvu wagonjwa, wala
hamkuwaponya wenye maradhi. Hamkuwafungua wale waliovunjika, hamkuwarud-
isha waliofukuzwa au kuwatafuta waliopotea. Badala yake, mmetawala juu yao
kwa nguvu na vurugu. 5 Kisha walikuwa wametawanyika bila mchungaji, na
wakawa chakula kwa wanyama wote waishio katika mashamba, walipokuwa
wametawanyika. 6 Kundi langu limetawanyika juu ya milima yote na juu ya kilima
kirefu, na limetawanyika juu ya uso wote wa dunia. Wala hakuna anayewatafua.
7 Kwa hiyo, wachungaji, sikilizeni neno la Yahwe: 8 Kama niishivyo-hivi ndivyo
Bwana Yahwe asemavyo-kwa sababu kundi langu limekuwa mateka na chakula
kwa ajili ya wanyama katika mashamba, kwa sababu hapakuwa na mchungaji
yeyote, lakini wachungaji walijilisha wenyewe na hawakulisha kundi langu. 9 Kwa
hiyo, wachungaji, lisikilizeni neno la Yahwe: 10 Bwana Yahwe asema hivi: Tazama!
Niko juu ya wachungaji, na nitalitaka kundi langu kutoka mkononi mwake. Kisha
nitawaachisha kutoka kulichunga kundi; wala wachungaji hawatajilisha wenyewe
tena kwa kuwa nitaliondoa kundi langu kutoka midomoni mwao, ili kwamba
kundi langu lisiwe chakula kwa ajili yao tena. 11 Kwa kuwa Bwana Yahwe
asema hivi: Tazama! mimi mwenyewe nitawatafuta kondoo wangu na kuwaulizia,
12 kama mchungaji atafutaye kundi lake juu ya siku hiyo yupo ndani ya kundi
lake lililotawanyika. Hivyo nitalitafuta kundi langu, na nitalichunga kutoka sehemu
lilipokuwa limetawanyika siku ya mawingu na giza. 13 Kisha nitalileta kutoka
miongoni mwa watu; nitalikusanya kutoka nchi mbali mbali na kulileta kwenye nchi
yao. Nitaliweka kwenye malisho juu ya pande za milima ya Israeli, karibu na vijito, na
katika kila makazi katika nchi. 14 Nitawaweka kwenye malisho mema; juu ya milima
ya Israeli itakuwa sehemu za malisho yao. Watalala chini huko katika sehemu nzuri
kwa ajili ya malisho, katika malisho mengi, na watalisha juu ya milima ya Israeli.
15 Mimi mwenyewe nitachunga kondoo wangu, na mimi mwenyewe nitawalaza
chini-hivi ndivyo Bwana Yahwe 16 asemavyo-Nitawatafuta waliopotea nitawarudisha
waliofukuzwa. Nitawafunga waliovunjika na kuwaponya kondoo waliougua lakini
wanene na wenye nguvu nitawaharibu. Nitawalisha kwa haki. 17 Hivyo sasa ninyi,
kundi langu-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-tazama, nitakuwa hakimu kati
ya kondoo na kondoo na kati ya kondoo dume na mbuzi dume. 18 Je! haitoshi
kulisha juu ya malisho mazuri, ambayo mtayakanyaga chini kwa miguu yenu kile

kilichobakia kwenye malisho; na kunywa kutoka maji masafi, ambayo hakuna budi
kuikanyaga mito kwa miguu yenu? 19 Kondoo zangu zitakula kile mlichokanyagwa
kwa miguu yenu, na kunywa maji yale mliyoyakanyaga kwa miguu yenu? 20 Kwa
hiyo Bwana Yahwe anawaambia hivi; Tazama! Mimi mwenyewe nitahukumu kati ya
wanene na waliokonda, 21 Kwa kuwa mmewasukuma kwa ubavu wenu na mabega,
na kuwapiga kwa pembe wadhaifu wote kwa pembe zenu hadi mtakapowatawanya
mbali kutoka kwenye nchi. 22 Nitaliokoa kundi langu na hawatakuwa mateka tena,
na nitahukumu kati ya kondoo mmoja na mwingine! 23 Nitaweka juu yao mchungaji
mmoja, mtumishi wangu Daudi. Atawachunga, atawalisha, na atakuwa mchungaji
wao. 24 Kwa kuwa mimi, Yahwe, nitakuwa Mungu wao, na mtumishi wangu Daudi
atakuwa mkuu kati yao-mimi, Yahwe, nimesema hivi. 25 Kisha nitafanya agano la
amani pamoja nao na kuwaondoa wanyama waovu kutoka kwenye nchi, ili kwamba
waishi salama katika jangwa na walale salama katika misitu. 26 Pia nitaleta baraka
juu yao na juu ya maeneo yazungukao kilima changu, kwa kuwa nitaleta manyunyu
kwa wakati wake. Haya yatakuwa manyunyu ya baraka. 27 Kisha miti ya shambani
itazaa matunda yake, na dunia itashindwa kuzaa matunda yake. Kondoo wangu
watakuwa salama katika nchi yao; kisha watajua ya kwamba mimi ni Yahwe, wakati
nitakazipovunja fito za kongwa zao, na wakati nitakapowalinda kutoka kwenye
mkono wa wale walio watumikisha. 28 Hawatakuwa mateka tena kwa mataifa, na
wanyama pori juu ya dunia hawatawameza tena. Kwa kuwa wataishi salama na
wala hakuna mtu atakayewatia hofu. 29 Kwa kuwa nitatengeneza sehemu ya kulimia
nzuri kwa ajili yao hivyo hawataangamia kwa njaa katika nchi, na mataifa hayataleta
matukano juu ya yao. 30 Kisha watajua kwamba mimi, Yahwe Mungu wao, niko
pamoja nao. Ni watu wangu, nyumba ya Israeli-hivi ndivyo Bwana Mungu asemavyo.
31 Kwa kuwa ninyi ni kondoo wangu, kundi la malisho yangu, na watu wangu, na
mimi ni Mungu wenu-hivi ndivyo Bwana Mungu asemavyo."

# 35

1 Kisha neno la Yahwe likanijia, kusema, 2 "Mwanadamu, weka uso wako juu ya
Mlima Seiri na tabiri dhidi yake. 3 Uiambie, 'Bwana Yahwe asema hivi: Tazama!
ni juu yako, Mlima Seiri, nitakupiga kwa mkono wangu na kukufanya ukiwa na
tishio. 4 Nitaiharibu miji yenu, na wewe mwenyewe utakuwa ukiwa; kisha utajua
kuwa mimi ni Yahwe. 5 Kwa sababu umekuwa adui kwa watu wangu Israeli siku
zote, na kwa sababu umewatoa kwenye mikono ya upanga wakati wa mateso yao,
wakati adhabu yao itakapokuwa katika ukubwa wake. 6 Kwa hiyo, kama niishivyo-
hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-nitaandaa kwa ajili ya damu, na damu na
kukufutilia! Kwa kuwa hukuchukia damu, damu itakufuatilia. 7 Nitaufanya Mlima
Seiri mkamilifu na ukiwa wakati nitakapoukatilia mbali kutoka huo yeyote apitaye
na arudiye tena. 8 Kisha nitaijaza milima kwa watu wao waliokufa. Milima yako na
mabonde na mifereji-wale walioawa kwa upanga wataanguka kati yao. 9 Nitakufanya
mkiwa daima. Miji yako haitakaliwa na watu, lakini mtajua kwamba mimi ni
Yahwe. 10 Umesema, "Haya mataifa mawili na hizi nchi mbili zitakuwa zangu,
na tutazimiliki," hata wakati Yahwe alipokuwa pamoja nao. 11 Kwa hiyo, kama
niishivyo-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-hivyo nitafanya kulingana na hasira
yako na kulingana na wivu wako ambao uliousikia katika chuki yako ya Israeli, na
nitajidhihirisha kwao nitakapokuhukumu. 12 Hivyo utajua kwamba mimi ni Yahwe.
Nimeyasikia matukano yako yote uliyasema dhidi ya milima ya Israeli, uliposema,
"Wameharibiwa; wametolewa kwetu tuwale. 13 "Nanyi mmejitukuza juu yangu kwa
kile mlichokisema, na mmeongeza maneno juu yangu; na kuyasikia yote. 14 Bwana
Yahwe asema hivi: Nitakufanya ukiwa, wakati dunia nzima itakapofurahi. 15 Kama

vile unavyofurahi juu ya urithi wa watu wa Israeli kwa sababu ukiwa ya wake,
ndivyo nitakavyokutenda wewe. Utakuwa ukiwa, Mlima Seiri, na Edomu yote! Kisha
watajua kwamba mimi ni Yahwe."'

# 36

1 "Na wewe, mwanadamu, itabirie milima ya Israeli na useme, 'Milima ya Israeli,
lisikilizeni neno la Yahwe. 2 Bwana Yahwe asema hivi: Adui amesema kuhusu
ninyi, "Aha!" na "Mahala pa juu pa zamani pamekuwa milki yetu."' 3 Kwa hiyo
tabiri na sema, 'Bwana Yahwe asema hivi: Kwa sababu ya ukiwa wenu na kwa
sababu mashambulizi yaliyokuja juu yenu kutoka pande zote, mmekuwa milki ya
mataifa mengine; mmeambiwa kwa midomo yao waongeao, na kwa masingizio
ya watu. 4 Kwa hiyo, milima ya Israeli, sikilizeni neno la Bwana Yahwe: Bwana
Yahwe asema hivi kwa milima na vilima, mifereji ya maji na mabonde, mahali
palipoharibika kuwa ukiwa na miji iliyoachwa ambayo imetekwa nyara na kutokuwa
huru kwa kutaniwa na mataifa yaliyowazunguka- 5 kwa hiyo Bwana Yahwe asema
hivi: Hakika nimeongea katika moto wa hasira yangu juu ya mataifa meningine,
juu ya Edemu na wote waliochukua nchi yangu kwa ajili yao wenyewe kama milki,
dhidi ya wale walikuwa na furaha yote katika mioyo yao na dharau katika roho
zao, kama walivyoitwaa nchi yangu kwamba wangeweza kudai nchi za malisho kwa
ajili yao. 6 Kwa hiyo, tabiri kwa nchi ya Israeli na sema kwa milima na vilima,
hata kwenye mifereji na mabonde, Bwana Yahwe asema hivi: Tazama! Katika
ghadhabu yangu na hasira yangu nasema hivi kwa sababu mmechukua fedheha
za mataifa. 7 Kwa hiyo, Bwana Yahwe asema hivi: Mimi mwenyewe nitainua
mkono wangu kuapa kwamba mataifa yanayowazunguka yamkini yatawabebea aibu
yao wenyewe. 8 Lakini ninyi, milima ya Israeli, mtachipuza matawi na kuzaa
matunda kwa ajili ya watu wangu Israeli, kwa kuwa watarudi kwenu. 9 Maana
tazama, nipo kwa ajili yenu, na kuwachukulia kwa fadhili; mtalimwa na kupandwa
mbegu. 10 Hivyo nitawaongeza juu ya milima yenu watu katika nyumba ya Israeli,
yote. Miji itakaa na palipoharibiwa kujengwa. 11 Nitaongeza mtu na wanyama
juu yenu milima ili kwamba itaongezeka na kuzaa. Kisha nitawafanya kuishi
kama mlivyokuwa, na nitawafanya kustawi zaidi kuliko mlivyokuwa zamani, kwa
kuwa mtajua yakwamba mimi ni Yahwe. 12 Nitawaleta watu, watu wangu Israeli,
kutembea juu yenu. Watakumiliki, na utakuwa urithi wao, na hutasababisha tena
watoto wao kufa. 13 Bwana Yahwe asema hivi: Kwa sababu wanakwambia, "Wewe
unakula watu, na watoto wa nchi yako wamekufa," 14 kwa hiyo hautawala watu
wangu tena, na hutalifanya tena taifa lako kuomboleza vifo vyao. Hivi ndivyo
Bwana Yahwe asemavyo. 15 Wala sintokuruhusu kusikiliza fedhiha za mataifa tena;
hautachukua tena aibu ya watu au kufanya taifa lako kuanguka-hivi ndivyo Bwana
Yahwe asemavyo."' 16 Kisha neno la Yahwe likanijia, kusema, 17 "Mwanadamu, wakati
nyumba ya Israeli walipoikalia nchi yao, waliinajisi kwa njia zao na matendo yao.
Njia zao zilikuwa kama uchafu wa hedhi ya mwanamke mbele yangu. 18 Hivyo
nilimwaga ghadhabu yangu juu yao kwa ajili ya damu ambayo waliyoimwaga juu ya
nchi na kwa ajili ya uchafu wa hiyo kwa sanamu zao. 19 Nimewatawanya miongoni
mwa mataifa; walitawanyika katika nchi nyingi. Nimewahukumu kulingana na njia
zao na matendo yao. 20 Kisha wakaenda kati ya mataifa, na popote walipoenda,
walilitukana jina langu takatifu wakati watu waliwasema, 'Je! hawa kweli ni watu
wa Yahwe? Kwa kuwa wamefukuzwa nje ya nchi yake. 21 Lakini nilikuwa na huruma
kwa ajili ya jina langu takatifu ambalo nyumba ya Israeli walilinajisi miongoni
mwa mataifa, walipoenda huko. 22 Kwa hiyo waambie nyumba ya Israeli, 'Bwana
Yahwe asema hivi: Sifanyi haya kwa ajili yenu, nyumba ya Israeli, lakini jina

langu, mlilolitukana miongoni mwa mataifa kila sehemu mlipoenda. 23 Kwa kuwa
nitalifanya jina langu kuu kuwa takatifu, mlilolitukana miongoni mwa mataifa-
katikati ya mataifa, mmelitukana. Kisha mataifa watajua kwamba mimi ni Yahwe-
hivi ndivyo asemavyo Bwana Yahwe-asemavyo-wakati mtakapoona kwamba mimi
ni mtakatifu. 24 Nitawachukua kutoka mataifa na kuwakusanya kutoka kila nchi,
na nitawaleta hata nchi yenu. 25 Kisha nitanyunyiza maji masafi juu yenu ili
muwe wasafi kutoka kwenye uchafu wote, na nitawasafisha kutoka sanamu zenu
zenu. 26 Nitawapatia moyo mpya na roho mpya sehemu zenu za ndani, na nitautoa
moyo wa jiwe kutoka kwenye nyama zenu. Kwa kuwa nitawapatia moyo wa
nyama. 27 Nitaiweka Roho yangu ndani yenu na kuwawezesha kutembea katika
sheria zangu na kuziweka hukumu zangu, hivyo mtazitenda. 28 Kisha mtakaa
katika nchi niliyowapa babu zenu; mtakuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu
wenu. 29 Kwa kuwa nitawaokoa kutokana na uchafu wenu wote. Nitaita ngano
kuiongeza. Sitaweka tena njaa juu yenu. 30 Nitaongeza tunda la mti na kuzalisha
kwenye mashamba ili kwamba msichukue tena aibu ya njaa juu ya mataifa. 31 Kisha
mtazikumbuka njia zenu mbaya na matendo yenu ambayo hayakuwa mazuri, na
mtaonyesha chuki kwenye nyuso zenu kwa sababu ya dhambi zenu na matendo yenu
maovu. 32 Sifanyi hili kwa ajili yenu-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-ijulikane
kwenu. Hivyo tahayarikeni na kufadhaika kwa sababu ya njia zenu, nyumba ya
Israeli. 33 Bwana Yahwe asema hivi: Katika siku niliyowatakasa kutoka kwenye uovu
wenu wote, nitawafanya miji ikaliwe na kuzijenga sehemu zilizoharibiwa. 34 Kwa
kuwa mtailima nchi iliyoharibiwa hadi itakapoonekana haijaaharibika mbele za
macho ya wote wapitao karibu. 35 Kisha watasema, “Hii nchi ilikuwa ukiwa, lakini
imekuwa kama bustani ya Edeni; miji ya ukiwa na isiyo na wakaaji iliyo magofu
ambayo ilibomolewa sasa inakaliwa. 36 Kisha mataifa mengine waliowazunguka
watajua yakwamba mimi ni Yahwe, kwamba nimejenga palipokuwa pameharibiwa
na kuipanda mbegu sehemu iliyokuwa ukiwa. 37 Bwana Yahwe asema hivi: Tena
nitaulizwa na nyumba ya Israeli kufanya hivi kwa ajili yao, kuwaongeza kama
kundi la watu. 38 Kama kundi lililotengwa kwa ajili ya sadaka, kama kundi katika
Yerusalimu katika sikukuu yake iliyoteuliwa, hivyo miji itaharibiwa kwa kujazwa na
makundi ya watu na watajua kwamba mimi ni Yahwe.”'

# 37

1 Mkono wa Yahwe ulikuwa juu yangu, na akanitoa kwa Roho wa Bwana Yahwe na
kuniweka chini katikati ya bonde; lilikuwa limejaa mifupa. 2 Kisha akanifanya kupita
kati yao kuizunguka pande zote. Tazama! Mingi yao mikubwa ilikuwa katika bonde!
Ilikuwa mikavu sana. 3 Akanambia, “Mwanadamu, Je! Hii mifupa inaweza kuishi
kinyume?” Hivyo nikasema, “Bwana Yahwe, wajua wewe pekee.” 4 Kisha akanambia,
“Tabiri juu ya hii mifupa na iambie, 'Mifupa mikavu. Lisikilizeni neno la Yahwe.
5 Bwana Yahwe asema hivi kwenye hii mifupa: Tazama! nakaribia kuweka pumzi
juu yenu, nanyi mtaishi. 6 Nitaweka mishipa juu yenu na kuleta nyama juu yenu.
Nitawafunika kwa ngozi na kuweka pumzi ndani yenu hivyo mtaishi. Kisha mtajua
kwamba mimi ni Yahwe.”' 7 Hivyo nimetoa unabii kama nilivyokuwa nimeamriwa:
nimetabiri, tazama, sauti ikaja, iliyokuwa ya mtetememo. Kisha mifupa ikasogeleana
pamoja-mfupa juu ya mfupa. 8 Nikatazama na, kumbe, mishipa ilikuwa juu sasa,
na nyama ikatoka juu na ngozi ikazifunika. Lakini hapakuwa na pumzi juu yao.
9 Kisha Yahwe akanambia, “Itabirie pumzi, tabiri, mwanadamu, na iambie pumzi,
'Bwana Yahwe asema hivi: Pumzi, hutoka pepo nne, na pumzi juu ya hawa walioawa,
hivyo wanaweza kuishi.”' 10 Hivyo nimetabiri kama nilivyokuwa nimeamriwa; pumzi
ikawajilia na wakaishi. Kisha wakasimama kwa miguu yao, jeshi moja kubwa sana.

[11] Kisha Yahwe akanambia, “Mwanadamu, mifupa hii yote ni ya nyumba ya Israeli.
Tazama! Wanasema, 'Mifupa yetu imekauka, na tumaini letu limepotea. Tumekatwa.'
[12] Kwa hiyo tabiri na waambie, 'Bwana Yahwe asema hivi: Tazama! Nitayafunua
makabiri yenu na kuwapandisha kutoka kwayo, watu wangu. Nitakurudisha hata
katika nchi ya Israeli. [13] Kisha mtajua kwamba mimi ni Yahwe, nitakapo yafunua
makaburi yenu na kuwatoa kutoka kwao, watu wangu. [14] Nitaweka Roho wangu
ndani yenu hivyo mtaishi, na nitawafanya kupumzika katika nchi yenu mtakapojua
yakwamba mimi ni Yahwe. Nasema na nitayafanya hayo-hivi ndivyo Bwana Yahwe
asemavyo.”' [15] Kisha neno la Yahwe likanijia, likisema, [16] “Sasa wewe, mwanadamu,
chukua fimbo moja kwa ajili yako na andika juu yake, 'Kwa ajili Yuda na kwa ajili
ya watu wa Israeli, wenzake,' Kisha fimbo nyingine andika juu yake, 'Kwa kuwa
Yusufu, tawi la Efraimu, na kwa ajili ya watu wa Israeli, wenzake. [17] Walete wote
pamoja kwenye fimbo moja, ili wawe kitu kimoja katika mkono wako. [18] Wakati
watu wako watakapokwambia na kusema, 'Je! hutatuambia haya mambo yako yana
maana gani?' [19] kisha waambie, 'Bwana Yahwe asema hivi: Tazama! Nalichukua
tawi la Yusufu ambalo lipo kwenye mkono wa Efraimu na kabila za Israeli wenzake
na kuungana nalo hata kwenye tawi la Yuda, ili kwamba wawe tawi moja, na
watakuwa kitu kimoja katika mikono yangu.' [20] Shika kwenye mkono wako na
matawi uliyoandika mbele ya macho yao. [21] Waambie, 'Bwana Yahwe asema hivi:
Tazama! nakaribia kuwachukua watu wa Israeli kutoka miongoni mwa mataifa
walipoenda. Nitawakusanya kutoka nchi zilizozunguka na nitawaleta kwenye nchi
yao. [22] Nitawafanya kuwa taifa moja katika nchi, juu ya milima ya Israeli, na
kutakuwa na mfalme mmoja kama mfalme juu yao wote, na hawatakuwa mataifa
mawili tena. Hawatagawanyika kwenye falme mbili tena. [23] Kisha hawatajitia
unajisi tena kwa sanamu zao, mambo yao yachukizao, au dhambi zao nyingine. Kwa
kuwa nitawaokoa kutoka matendo yao ya uongo ambayo wamefanya dhambi, na
nitawatakasa, hivyo watakuwa watu wangu nami nitakuwa Mungu wao. [24] Daudi
mtumishi wangu atakuwa mfalme juu yao. Hivyo kutakuwa na mchungaji mmoja
juu yao wote, na wataishi kulingana na sheria zangu na watazitunza amri zangu na
kuzitii. [25] Wataishi katika nchi niliwapatia watumishi wangu Yakobo, ambapo baba
zenu walipoishi. Wataishi humo milele-wao, watoto wao, na wajukuu zao, kwa Daudi
mtumishi wangu atakuwa mkuu wao milele. [26] Nitaweka agano la amani pamoja nao.
Litakuwa agano la milele pamoja nao. Nitawaweka na kuwazidisha na kupaweka
mahali patakatifu pangu katikati yao milele. [27] Maskani yangu yatakuwa pamoja
nao; Nitakuwa Mungu wao, na watakuwa watu wangu. [28] Kisha mataifa watajua
yakwamba mimi ni Yahwe niliyewatenga Israeli, wakati mahali pangu patakatifu
patakapokuwa katikati yao milele.”

# 38

[1] Neno la Yahwe likanijia, likisema, [2] “Mwanadamu, weka uso wako kumwelekea
Gogu, nchi ya Magogu, kiongozi mkuu wa Mesheki na Tubali; na kutabiri dhidi
yake. [3] Sema, 'Bwana Yahwe asema hivi: Tazama! Ni juu yako, Gogu, kiongozi
mkuu wa Mesheki na Tubali. [4] Hivyo nitakugeuza na kuweka kulabu kwenye taya
yako; nitakupeleka nje pamoja na jeshi lako lote, farasi, na waendesha farasi, wote
wakiwa wamevaa silaha, kusanyiko kubwa pamoja na ngao ndogo na ngao kubwa,
wote wakishikilia panga! [5] Persia, Kushi, Uajemi wapo pamoja nao, wote pamoja
na ngao na chapeo! [6] Gomeri na jeshi lake lote, na Beth-Togarma, kutoka sehemu
za mbali ya kaskazini, na jeshi lake lote! Watu wengi wako pamoja nawe! [7] Kuwa
tayari! Ndio, jiandae na jeshi lako waliokusanyika pamoja na wewe, na amiri wao
mkuu. [8] Utaitwa baada ya siku nyingi, na baada ya miaka michache utaenda kwenye

nchi iliyofunikwa kutoka upanga na ambayo iliyokusanywa kutoka watu wengi,
iliyowkusanya kuwarudisha milima ya Israeli ambayo imeendelea kuangamizwa.
Lakini watu wa nchi watatolewa na kabila za watu, na wataishi salama, wote!
9 Hivyo utapanda juu kama tufani iendavyo; utakuwa kama wingu lililofunika nchi,
wewe na jeshi lako lote, maaskari wako wote pamoja na wewe. 10 Bwana Yahwe
asema hivi: Itakuwa siku hiyo hayo mawazo yataingia moyoni mwako, na utatunga
njama mbaya.' 11 Kisha utasema, 'nitapanda hata nchi iliyowazi; nitaenda hata
kwa watu wapole waishio salama, wote wakiishi mahali ambapo hakuna kuta wala
makomeo, na mahali ambapo hakuna malango ya mji. 12 Nitanyakua mateka na
kuiba mateka, ili nilete mkono wangu juu kuwaangamiza wale wakazi wapya, na juu
ya watu waliokusanyika kutoka mataifa, watu wale waongezao wanyama na mali,
na wale waishio katikatika ya dunia.' 13 Sheba na Denani, na wafanya biashara wa
Tarshishi pamoja na mahodari wake wote watakwambia, 'Je, umekuja kuteka nyara?
Je, umewakusanya majeshi yako kuchukua mateka, kuchukua fedha na dhahabu,
kuchukua mifugo yao na mali na kuwakokota mateka wengi sana?' 14 Kwa hiyo
tabiri, mwanadamu, na mwambie Gogu, 'Bwana Yahwe asema hivi: Katika siku
hiyo, wakati watu wangu Israeli watakapoishi salama, je, hutajifunza kuhusu wao?
15 Utakuja kutoka mahali pangu mbali katika kaskazini pamoja na jeshi kubwa,
wote wakiendesha farasi, kusanyiko kubwa, jeshi kubwa. 16 Utawashambulia watu
wangu Israeli kama wingu lifunikavyo nchi. Katika siku za baadaye nitakuleta
juu ya nchi yangu, ili mataifa wanijue nitakapojifunua mwenyewe kupitia wewe,
Gogu, kuwa mtakatifu mbele ya macho yao. 17 Bwana Yahwe asema hivi: Je,
wewe siye yule ambaye niliyeongea naye katika siku za zamani kwa mkono wa
watumishi wangu, manabii wa Israeli, waliotabiri katika mda wao wenyewe kwa
miaka niliyowaleta juu yao? 18 Basi itakuwa katika siku hiyo wakati Gogu atakapo
ishambulia nchi ya Israeli-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-ghadhabu yangu
itapanda katika hasira yangu. 19 Katika wivu wangu katika hasira ya moto wangu,
ninasema kwamba katika siku hiyo kutakuwa na tetemeko kubwa la nchi katika nchi
ya Israeli. 20 Watatetemeka mbele yangu-samaki wa baharini na ndege wa angani,
wanyama wa mashambani, na viumbe watambaao juu ya nchi, na kila mtu aliyeko
juu ya uso wa nchi. Milima itaangushwa chini majabali yataanguka, hadi kila ukuta
utaanguka kwenye nchi. 21 Nitaita upanga dhidi yake juu ya milima yangu yote-hivi
ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-upanga wa kila mtu utakuwa kinyume na ndugu
yake. 22 Kisha nitamuhukumu kwa tauni na damu; nakufurika mvua na mvua ya
mawe na kuchoma asidi nitainyeshea chini juu yake na jeshi lake na mataifa mengi
yaliyo pamoja naye. 23 Kwa kuwa nitaonyesha ukuu wangu na utakatifu wangu na
nitafanya kujulikana mimi mwenyewe katiaka macho ya mataifa mengi, na watajua
kwamba mimi ni Yahwe."

# 39

1 "Kisha wewe, mwanadamu, tabiri dhidi ya Gogu na sema, 'Bwana Yahwe asema
hivi: Tazama! ni kinyume nawe, Gogu, mkuu wa Mesheki na Tubali. 2 Nitakugeuza
na kukuongoza; nitakupandisha juu kutoka mbali kaskazini na kukuleta hata milima
ya Israeli. 3 Kisha nitaufunga upinde wako utoke katika mkono wako wa kushoto
na kuifanya mishale kuanguka kutoka kwenye mkono wako wa kuume. 4 Utaanguka
juu ya milima ya Israeli-wewe na jeshi lako late na maaskari walio pamoja nawe.
Nitawapatia ndege mbua na wanyama pori wa mashambani kwa ajili ya chakula.
5 Utaanguka juu ya uso wa shamba, kwa kuwa mimi mwenyewe nimesema hivyo-
hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. 6 Kisha nitapeleka moto juu ya Magogu na
kwa wale waishio salama juu ya pwani, na watajua yakwamba mimi ni Yahwe.

7 Kwa kuwa nitalifanya jina langu takatifu lijulikane kati ya watu wangu Israeli,
na sitaruhusu tena jina langu takatifu litukanwe; mataifa watajua kwamba mimi
ni Yahwe, Mtakatifu katika Israeli. 8 Tazama! Siku inakuja, na itachukua nafasi-
hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. 9 Hao wakaao katika miji ya Israeli watatoka
nje na watatumia silaha kuwasha moto na kutengeneza moto na kuwachoma-ngao
ndogo, ngao kubwa, pinde, mishale, rungu, na mikuki; watatengeneza mioto pamoja
nao kwa muda wa siku saba. 10 Hawatakusanya kuni kutoka mashambani wala
kukata miti kutoka kwenye misitu, kwa kuwa watazichoma hizo silaha; watawateka
nyara wale watakaotaka kuwateka nyara-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo."
11 Kisha itakuwa katika hiyo siku ambayo nitaifanya sehemu huko kwa ajili ya Gogu-
kaburi la Israeli, bonde kwa ajili ya wale wanaosafiri hata mashariki ya bahari.
Litawazuia wale wanaotegemea kupita. Huko watamzika Gogu pamoja na kundi
lake lote. Watapaita bonde la Hamon-Gogu. 12 Kwa muda wa siku saba nyumba
ya Israeli itawazika ili kuitakasa nchi. 13 Kwa kuwa watu wa nchi watawazika;
itakuwa siku ya kukumbukwa kwao wakati nitakapotukuzwa-hivi ndivyo Bwana
Yahwe asemavyo. 14 Kisha watawateua watu kuendelea kwenda kwenye nchi,
kuwatafuta wale waliokuwa wakisafiri, lakini waliokufa na miili yao kubaki juu
ya uso wa nchi, ili kwamba waweze kuwazika, kwa ajili ya kusafisha nchi. Katika
siku ya mwisho ya mwezi wa saba wataanza kutafuta. 15 Kama hawa watu wapitao
kwenye nchi, watakapoona mfupa wowote wa binadamu, wataweka alama kwa
huo, hadi wachimba kaburi watakapokuja na kuizika katika bonde la Hamoni
Gogu. 16 Kutakuwa na mji huko unaitwa Hamona. Wataitakasa nchi kwa njia hii.
17 Kwako wewe, mwanadamu, Bwana Yahwe asema hivi: Waambie ndege wote
wenye mabawa na wanyama wote wa porini katika mashamba, 'Kusanyikeni pamoja
na mje. Kusanyikeni kutoka pande zote kwenda kwenye dhabihu yote ambayo
mimi mwenyewe ninayoifanya kwa ajili yako, dhabihu kubwa juu ya milima ya
Israeli, ili kwamba mle nyama na kunywa damu. 18 Mtakula nyama ya walio
hodari na kunywa damu ya wakuu wa dunia; watakuwa kondoo waume, wana
kondoo, mbuzi, na ng'ombe, wote walikuwa wanene katika Basheni. 19 Kisha mtakula
mafuta hata kuridhika kwenu; mtakunywa damu hadi kulewa; hii itakuwa dhabihu
nitakayoichinja kwa ajili yenu. 20 Mtatosheka kwenye meza yangu pamoja na farasi,
magari ya farasi, shujaa, na kila mtu wa vita-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo.'
21 Nitauweka utukufu wangu kati ya mataifa, na mataifa yote yataona hukumu yangu
ninayoionyesha na mkono wangu nimeuweka juu yao. 22 Nyumba ya Israeli itajua
yakwamba mimi ni Yahwe Mungu wao kutoka hiyo siku na kuendelea. 23 Mataifa
yatajua kwamba nyumba ya Israeli wameenda uhamishoni kwa sababu ya udhalimu
wao kwa kunisaliti, hivyo naficha uso wangu kwao na kuwaweka kwenye mkono
wa maadui zao ili kwamba wote waanguke kwa upanga. 24 Nimewafanyia kutokana
na uchafu wao na dhambi zao, nitakapokuwa nimeuficha uso wangu kwao. 25 Kwa
hiyo Bwana Yahwe asema hivi: Sasa nitawarudisha watu wa Yakobo, na kuwa na
huruma juu ya nyumba yote ya Israeli, wakati nitakapoona wivu kwa ajili ya jina
langu. 26 Kisha watabeba aibu yao na uhaini mkubwa walio nihaini. Watayasahau
haya yote watakapopumzika katika nchi yao katika usalama, wala hakuna mtu
atakaye waogofya. 27 Wakati nitakapokuwa nimewarudisha kutoka kwa watu na
kuwakusanya kutoka kwenye nchi za maadui zao, nitajionyesha mimi mwenyewe
kuwa mtakatifu kwenye uso wa mataifa mengi. 28 Kisha watajua kwamba mimi ni
Yahwe Mungu wao, kwa kuwa nimewapeleka utumwani kati ya mataifa, lakini kisha
nitawakusanya kuwarudisha hata nchi yao. Sitamuacha hata mmoja wao kati ya
mataifa. 29 Sitawaficha uso wangu kwao wakati nitakapomwaga Roho wangu katika
nyumba ya Israeli-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo."

# 40

[1] Katika mwaka wa ishirini na tano wa kuhamishwa kwetu mwanzoni mwa mwaka
siku ya kumi ya mwezi, katika mwaka wa kumi na nne baada ya mji kuchukuliwa-
katika siku hiyo hiyo, mkono wa Yahwe ulikuwa juu yangu na alinichukua huko.
[2] Katika maono ya Mungu akanileta hata nchi ya Israeli. Akanileta kupumzika
juu ya kila mlima mrefu sana; upande wa kusini kulikuwa na monekano kana
kwamba majengo ya mji. [3] Kisha akanileta huko. Tazama, kulikuwa na mtu!
Mwonekano wake ulikuwa kama mwonekano wa shaba. Alikuwa na uzi wa kitani na
mwanzi wa kupimia mkononi mwake, na alisimama katika lango la mji. [4] Huyo mtu
akanambia, “Mwanadamu, tazama kwa macho yako na sikiliza kwa masikio yako, na
elekeza moyo wako juu ya yote ninayokufunulia, kwa kuwa ulinileta hapa ili niweze
kukufunulia haya wewe. Toa taarifa ya kila kitu utakachokiona kwa nyumba ya
Israeli. [5] Kulikuwa ukuta uliokuwa umezunguka eneo la hekalu. Urefu wa kipimo
cha mwanzi katika mkono wa mtu ulikuwa dhiraa sita urefu, kila urefu wa dhiraa
ulikuwa dhiraa moja na kipimo cha kiganja cha mkono urefu. Aliupima ukuta;
ulikuwa kipimo cha mwanzi mmoja na ufito mmoja urefu. [6] Kisha akaenda hata
kwenye lango la hekalu lililokuwa limeelekea mashariki. Akapanda ngazi na kuipima
kizingiti cha lango-mwanzi mmoja upana. [7] Vyumba vya ulinzi vilikuwa kila mwanzi
mmoja urefu na mwanzi mmoja upana; kulikuwa na dhiraa tano katika kila vyumba
viwili, na kizingiti cha lango la hekalu karibu na tawa la hekalu kilikuwa mwanzi
mmoja urefu. [8] Akapima tawa la lango; ulikuwa mwanzi mmoja urefu. [9] Akapima
tawa la lango. Ilikuwa mwanzi mmoja kwenda chini. Mihimili ilikuwa dhiraa mbili
upana. Hili lilikuwa tawa la lango kuelekea hekalu. [10] Kulikuwa na vyumba vitatu vya
ulinzi pande zote za lango la mashariki, na yote yalikuwa na kipimo kile kile, na kuta
zilizokuwa zimezigawanya zilikuwa na kipimo kile kile. [11] Kisha yule mtu akapima
upana wa njia ya lango la kuingia-dhiraa kumi; na akapima urefu wa njia ya lango la
kuingia-dhiraa kumi na tatu. [12] Akaupima ukuta uliokuwa mpaka mbele ya vyumba-
dhiraa moja urefu. Vyumba vilipimwa dhiraa sita kila upande. [13] Kisha akapima
lango la njia kutoka kwenye paa ya chumba kimoja kuelekea chumba kingine-dhiraa
ishirini na tano, kutoka lango la kuingia chumba cha kwanza kuelekea kile cha pili.
[14] Kisha akapima ukuta uliokuwa umeenda kati ya vyumba vya ulinzi-dhiraa sitini
urefu; alipima kwa mbali na tawa la lango. [15] Lango la kuingia kutoka lango la mbele
kuelekea lango jingine la tawa la mwisho lilikuwa dhiraa hamsini. [16] Kulikuwa na
madirisha yaliyokuwa yamefungwa kuelekea vyumba na kuelekea nguzo zake kati
ya malango kuzunguka kote; na vivyo hivyo kwa mabaraza. Kulikuwa na madirisha
pande zote za ndani, na kila mhimili ulikuwa umepambwa kwa mitende. [17] Kisha
huyo mtu akanileta hata ua wa nje mwa hekalu. Tazama, kulikuwa na vyumba, na
kulikuwa na kibamba katika ua, pamoja na vyumba thelathini baada ya kibamba.
[18] Kibamba kilienda juu hata upande wa malango, na upana wake ulikuwa sawsawa
na urefu wa malango. Hiki kilikuwa kibamba cha chini. [19] Kisha huyo mtu akapima
umbali kutoka mebele ya lango la chini hata mbele ya lango la ndani; ilikuwa dhiraa
mia moja upande wa mashariki, na sawasawa na upande wa kaskazini. [20] Kisha
akapima urefu na upana wa lango lililokuwa upande wa kaskazini mwa ua wa
nje. [21] Kulikuwa na vyumba vitatu pande zote za lango, na lango na matawa yake
yalipimwa sawa na lango kubwa-dhiraa hamsini upana wote na dhiraa ishirini na
tano upana. [22] Madirisha yake, tawa, vyumba, na mitende yake vilikabiliana na lango
ambalo linaloelekea mashariki. Ngazi saba kuupandia juu hata kwenye tawa lake.
[23] Kulikuwa na lango kwenye ua wa ndani mbele kuelekea mashariki; huyo mtu
alipima kutoka lango moja hadi lango jingine-dhiraa mia moja umbali. [24] Kisha huyo
mtu akanileta hata kwenye lango la kuingia la kusini, na kuta zake na tawa vilipimwa

sawa kama malango mengine ya nje. 25 Kulikuwa na madirisha yaliyofungwa katika
lango la njia na tawa lake kama lile lango. Lango la kusini na tawa lake vilipimwa
dhiraa hamsini urefu na dhiraa ishirini na tano upana. 26 Kulikuwa na ngazi saba
hadi kwenye lango na matawa yake, na kulikuwa na mitende iliyochongoka juu ya
kuta pande zote. 27 Kulikuwa na lango la ua wa ndani upande wa kusini, na yule
mtu akapima kutoka hilo lango hata lango la kuingia upande wa kusini-dhiraa mia
moja umbali. 28 Kishi huyo mtu akanileta hata ua wa ndani karibu na lango lake la
kusini, ambalo lilikuwa na vipimo vile vile kama malango mengine. 29 Vyumba vyake,
kuta, na matao vilipimwa sawa kama malango mengine; kulikuwa na madirisha
kuzunguka matao yote. Lango la ndani na matao yake yalipimwa dhiraa hamsini
urefu na dhiraa ishirini na tano upana. 30 Pia kulikuwa na matao pande zote za
kuta za ndani; haya yalikuwa dhiraa ishirini na tano urefu na dhiraa tano upana.
31 Hili tawa lilielekea ua wa nje pamoja na mitende iliyochongwa juu ya kuta zake
na ngazi nane kuupandia. 32 Kisha yule mtu akanileta hata kwenye ua wa ndani
karibu na njia ya kaskazini na kulipima lango, ambalo lilikuwa na vipimo sawa
kama malango mengine. 33 Vyumba vyake, kuta, na matawa yalikuwa na kipima
sawa kama cha malango, na kulikuwa na madirisha pande zote. Laango la ndani
na matawa yake yalikuwa dhiraa hamsini urefu na dhiraa ishirini na tano upana.
34 Matawa yake yalielekea nje ya ua; ilikuwa na mitende pande zote za hiyo na
ngazi nane za kuupandia. 35 Kisha huyo mtu akanileta hata lango la kaskazini
na kulipima; likapimwa vivyo hivyo kama malango mengine. 36 Vyumba vyake,
kuta, na ukumbi vilipimwa sawa na malango mengine, na kulikuwa na madirisha
pande zote. Njia ya lango na matao yake yalipimwa dhiraa hamsini urefu na upana
dhiraa ishirini na tano. 37 Tatawa lake lilielekea ua wa nje; ilikuwa na mitende
pande zote za huo na ngazi nane kuupandia. 38 Kulikuwa na chumba pamoja na
mlango karibu na kila lango la ndani. Hapa ndipo ambako walipooshea sadaka za
kutekezwa. 39 Kulikuwa na meza mbili kila upande wa kila ukumbi, ambako sadaka
ya kuteketezwa ilipochinjiwa, na pia sadaka ya dhambi na sadaka ya hatia. 40 Karibu
na ukuta wa ua, kuelekea juu kwenye lango kuelekea kaskazini, kulikuwa na meza
mbili. Pia kwa upande mwingine kulikuwa na meza mbili kwenye lango la ukumbi.
41 Kulikuwa na meza nne pande zote karibu na lango; wakachinja wanyama juu ya
meza nane. 42 Kulikuwa na meza nne za mawe yaliyochongwa kwa ajili ya sadaka
ya kuteketezwa, dhiraa moja na nusu urefu, dhiraa moja na nusu upana, na kimo
dhiraa moja. Juu yake waliweka vyombo pamoja ambavyo walivichinjia sadaka za
kuteketezwa kwa ajili ya sadaka. 43 Kulabu mbili ujazo wa kiganja urefu uliokuwa
umeunganishwa katika ua pande zote, na nyama ya matoleo ilikuwa imewekwa juu
ya meza. 44 Karibu na lango la ndani, katika ua wa ndani, kulikuwa na vyumba vya
waimbaji. Moja ya hivi vyumba kilikuwa upande wa kaskazini, na kingine kusini.
45 Kisha yule mtu akanambia, “Hiki chumba kinachoelekea kusini ni kwa ajili ya
makuhani walio zamu katika hekalu. 46 Chumba kilichoelekea kaskazini kilikuwa
kwa ajili ya makuhani waliokuwa zamu kwenye madhabahu. Hawa ni wana wa
Sadoki ambaye huja humkaribia Yahwe kumtumikia; ambao ni miongoni mwa wana
wa Lawi.” 47 Kisha akaupima ule ua-dhiraa mia moja urefu na dhiraa mia moja upana
mraba, pamoja na madhabahu mbele ya nyumba. 48 Kisha yule mtu akanileta hata
kwenye varanda ya nyumba na kupima mwimo wa milango yake-ilikuwa dhiraa tano
unene upande huu. Njia ya kuingilia yenyewe ilikuwa dhiraa kumi na nne, na kuta
pande zote za huo zilikuwa dhraa tatu upana. 49 Urefu wa ukumbi ulikuwa dhiraa
ishirini, na upana wake ulikuwa dhiraa kumi na moja. Kulikuwa na ngazi zilizokuwa
zimepanda juu na nguzo zilizokuwa zimesimama pande zote za huo.

# 41

1 Kisha yule mtu akanileta mahali patakatifu pa hekalu na mihimili-dhiraa sita
upana pande zote. 2 Upana wa maingilio ulikuwa dhiraa kumi; ukuta kila upande
dhiraa tano urefu kila upande. Kisha yule mtu akapima ukubwa wa mahali
patakatifu-dhiraa arobaini upana urefu na dhiraa ishirini upana. 3 Kisha yule
mtu akaenda hata mahali patakatifu sana na kuipima miimili ya matokeo-dhiraa
mbili-kuta pande zote zilikuwa dhiraa saba upana. 4 Kisha akapima urefu wa
vyumba-dhiraa ishirini. Upana wake-dhiraa ishirini hata mbele kwenye ukumbi
wa hekalu. Kisha akanambia, “Hapa ndipo mahali patakatifu sana.” 5 Kisha yule
akapima kuta za nyumba-zilikuwa dhiraa sita unene. Upana wa kila upande wa
chumba kuzunguka nyumba dhiraa nne upana. 6 Kulikuwa na pande tatu za
vyumba, chumba kimoja juu ya kingine, vyumba thelathini, kulikuwa na kibao
kitokezacho ukutani kuzunguka ukuta wa nyumba, kusaidia pande zote za vyumba,
kwa kuwa hapakuwa na msaada uliokuwa umewekwa kwenye ukuta wa nyumba.
7 Hivyo mbavu za nyumba zilipanuka na kuzunguka kwenda juu, kwa kuwa nyumba
ilizunguka kwenda juu, na ngazi kuelekea juu hata sehemu ya juu, kupitia sehemu
ya katikati. 8 Kisha nikaona sehemu iliyoinuka kuzunguka nyumba, msingi kwa ajili
ya pande za vyumba; ikapimwa fimbo nzima urefu-dhiraa sita. 9 Upana wa ukuta
wa vyumba vya pembeni kwa upande wa nje ulikuwa dhiraa tano. Kulikuwa na
sehemu ya wazi kwa upande wa nje wa hivi vyumba katika patakatifu. 10 Kwa upande
mwingine wa hii sehemu ya wazi kulikuwa na vyumba vya makuhani upande wa nje;
hii sehemu ilikuwa na dhiraa ishirini upana kupazunguka patakatifu. 11 Kulikuwa
na milango kwenye vyumba vya pembeni kutoka sehemu ya wazi nyingine-njia
ya mlango moja uliokuwa upande wa kaskazini, na mwingine upande wa kusini.
Upana wa hili eneo la wazi ulikuwa na dhiraa tano kupazunguka. 12 Lile jengo
lililokuwa limeelekea kwenye ua upande wa magaribi dhiraa sabini upana. Ukuta
wake ulipimwa dhiraa tano pande zote, na ilikuwa dhiraa tisini urefu. 13 Kisha
yule mtu akapapima patakatifu-dhiraa mia moja urefu. jengo lililokuwa limetengeka,
kuta zake, na kwenye ua pia palipimwa dhiraa mia moja urefu. 14 Upana wa mbele
kwenye ua mbele ya patakatifu pia kulikuwa dhiraa mia moja. 15 Kisha yule mtu
akapima urefu wa jengo karibu na patakatifu, kwa upande wake wa magharibi, na
juu ya baraza pande zote-dhiraa mia moja. Mahali patakatifu na varanda, 16 kuta
za ndani na madirisha, pamoja na madirisha madogo, na baraza za pande zote
kwenye pande tatu, zilikuwa zimefungwa kwa mbao. 17 Juu ya lango la kuingilia
hata patakatifu pa ndani na kuwekwa karibu na kuta kulikuwa na pazia lililokuwa
limepimwa. 18 Palikuwa pamepambwa na makerubi mitende; pamoja na mitende
kati ya kerubi na kerubi, na kila kerubi lilikuwa na nyuso mbili: 19 uso wa mtu
aliyekuwa ameelekea mtende mmoja, na uso wa mwana simba ulitazama kuelekea
mtende kwa upande mwingine. Vilifunikwa kuzunguka malango ya kuingia yote
ya nyumba. 20 Kutoka chini hata juu kwenye njia ya mlango, makerubi na mtende
vilifunikwa na ukuta wa nje ya nyumba. 21 Mihimili ya lango la mahali patakatifu
lilikuwa mraba. Umbo lao lilikuwa kama umbo la 22 kwanza madhabahu ya mbao
mbele ya mahali patakatifu, ambapo kulikuwa na dhiraa tatu kwenda juu na dhiraa
urefu kwa kila upande. Pembe zake mihimili, kitako, na kiunzi kilitengenezwa kwa
mbao. Kisha yule mtu akanambia, “Hii ni meza ambayo itakuwa kwa ajili ya Yahwe.”
23 Kulikuwa na milango miwili kwa ajili ya mahali patakatifu na mahali patakatifu
sana. 24 Hii milango ilikuwa na bawaba mbili kila mlango paneli, paneli mbili kwa
ajili ya mlango mmoja na paneli mbili kwa ajili ya mwingine. 25 Ilifunikwa-juu
ya milango ya mahali patakatifu ambapo makerubi na mti wa mtende kama kuta
ilipambwa, kulikuwa na paa ya mbao juu ya varanda kwa mbele. 26 Kulikuwa na

madidsha madogo miti ya mitende kwenye varanda pande zote. Hivyo vilikuwa vyumba vya pembeni ya nyumba, na pia ilizielekea dari.

# 42

1 Kisha yule mtu akanituma kwenda ua wa nje upande wa kaskazini, akanileta kwenye vyumba mbele ya ua wa nje na ukuta wa nje kaskazini.
2 Hivyo vyumba vilikuwa dhiraa mia moja karibu na mbele yake na dhiraa hamsini upana.
3 Baadhi ya hivyo vyumba vilielekea ua wa ndani na vilikuwa na dhiraa ishirini kutoka patakatifu. Kulikuwa na vyumba vitatu vinavyolingana, na kingine juu kilichokuwa kimetazama chini kuelekea kingine vilikuwa vimefunguliwa, vilikuwa na pakutokea. Baadhi ya vyumba vilielekea nje kwenye ua wa nje.
4 Njia dhiraa kumi upana dhiraa mia moja urefu kueleikea mbele ya vyumba. Milango ya vyumba ilikuwa mbele kaskazini.
5 Lakini kumbi za juu zilikuwa ndogo, kwa ajili ya njia za kutembea zilichukua kutoka kwazo sehemu kubwa kulikuwa walivyofanya kwenye vyumba vya chini na katikati usawa wa jengo.
6 Kwa kuwa orofa tatu hapakuwa na mihimili, kama zile nyua, ambazo zilikuwa na mihimili. Hivyo usawa wa vyumba vya juu vilikuwa sawa sawa katika kipimo cha kulinganisha na vyumba vya chini na usawa wa katikakati.
7 Ukuta wa nje karibu na vyumba mbele ya ua wa nje, ua uliokuwa mbele ya vyumba. Huo ukuta ulikuwa dhiraa hamsini urefu.
8 Urefu wa vyumba vya ua wa nje ulikuwa dhiraa hamsini, na vyumba vilivyokuwa vimeelekea patakatifu vilikuwa dhiraa mia moja urefu.
9 Kulikuwa na mahali pa kuingilia kwenye vyumba vidogo zaidi kutoka upande mashariki, kuingia kutoka ua wa nje.
10 Karibu na ukuta wa ua wa nje juu ya upande wa mgaribi pa ua wa ndani, mbele ya patakatifu pa ua wa nje, pia kulikuwa na vyumba na njia ya mbele yao.
11 zilikuwa kama umbo la vyumba kwa upande wa kaskazini. Zilikuwa urefu ule ule na upana na matokeo yale yale na mipangilio na madirisha.
12 Kwa upande wa kusini kulikuwa na madirisha kwenye vyumba ambavyo vilikuwa kama yale yaliyokuwa upande wa kaskazini. Aya iliyokuwa ndani ilikuwa na mlango kwenye kichwa chake, na njia ilifunguliwa kwenye vyumba tafauti. Upande mashariki kulikuwa na malango wa njia kwenye njia mwishoni.
13 Kisha yule mtu akanambia, “Vyumba vya kaskazini na vyumba vya kusini vilivyokuwa mbele ya ua wa nje ni vyumba vitakatifu amabapo makuhani wafanyao kazi karibu sana na Yahwe waweze kula chakula kitakatifu sana. Wataweka vitu vitakatifu sana-sadaka ya chakula, sadaka ya dhambi, na sadaka ya hatia-kwa kuwa hapa ni mahali patakatifu.
14 Wakati makuhani watakapoingia hapo, wasitoke nje ya mahali patakatifu kwa ua wa nje, bila kuweka mavazi karibu mahali wahudumupo, kwa kuwa hapa ni patakatifu. Hivyo watavalia mahali pengine nguo kabla ya kwenda karibu na watu.”
15 Yule mtu akamaliza kupima ndani ya nyumba na kisha akanichukua nje ya lango lililokuwa limeelekea magharibi na kuzipima sehemu zote zilizokuwa zimepazunguka hapo.
16 Akaupima upande wa mashariki na fimbo ya kupimia-dhiraa mia tano kwa fimbo ya kupimia.
17 akaupima upande wa kaskazini-dhiraa mia tano na fimbo ya kupimia.
18 Pia akaupima upande wa kusini dhraa mia tano na fimbo ya kupimia.
19 Pia akageuka na kuupima upande wa magharibi dhiraa mia tano kwa fimbo ya kupimia,
20 Akaipima pande nne. Ilikuwa na ukuta umeizunguka ilikuwa dhiraa mia tano urefu, na dhiraa mia tano upana, kulitenganisha umbo takatifu kutoka ambapo ni pa kawada.

# 43

1 Yule mtu kisha akanileta hata kwenye lango lililokuwa linaelekea mashariki.
2 Tazama! Utukufu wa Mungu wa Israeli ukaja kutoka mashariki; sauti yake ilikuwa kama sauti ya maji mengi, na nchi iling'aa kwa utukufu wake.
3 Yalikuwa

yanalingana na sura ya ono nililolona, kulingana na ono nililokuwa nimeliona wakati
alipokuja kuuteketeza mji, na maono yalikuwa kama maono ambayo niliyokuwa
nimeyaona Keberi Kanali nikaanguka kifudi fudi. 4 Hivyo utukufu wa Yahwe
ukaja kwenye nyumba ya karibu na njia ya lango lililokuwa wazi kwa upande
wa magharibi. 5 Kisha Roho akanichukua na kunileta kwenye ua wa ndanni.
Tazama! Utukufu wa Yahwe ulikuwa umeijaza nyumba. 6 Mtu alisimama karibu na
mimi, na nikamsikia mtu mwingine akizungumza na mimi kutoka kwenye nyumba.
7 Akanambia, "Mwanadamu, hapa ndipo mahali pangu pa enzi na mahali kwa ajili ya
ya miguu yangu, ambapo nitaishi kati ya watu wa Israeli milele. Nyumba ya Israeli
haitalikufuru tena jina langu takatifu-wao au wafalme wao katika mahali patakatifu
pao. 8 Hawatalikufuru tena jina langu takatifu kwa kuweka kizingiti chao karibu
na kizingiti changu, na nguzo yao ya lango karibu na nguzo yangu ya lango, bila
kitu lakini ukuta kati yangu na wao. Wamelikufuru jina langu kwa matendo yao
machafu, hivyo nimewala kwa hasira yangu. 9 Sasa waache waondoe udanganyifu
wao na maiti za wafalme wao kutoka kwangu, na nitaishi katikati yao milele.
10 Mwanadamu, wewe mwenyewe utaiambia nyumba ya Israeli kuhusu nyumba hii
hivyo watajiskia aibu ya uovu wao. Wanaweza kutafakari kuhusu haya maelezo.
11 Kwa kuwa wameaibika kwa yote waliyoyafanya, kisha waonyeshe mchoro wa
nyumba, maelezo yake, matokeo yake, maingio yake, na mchoro wake, sheria zake
zote na kanuni. Kisha andika hivi chini mbele ya macho yao ili waweze kutunza
michoro yote na kanuni zake zote, hivyo kama wazitiivo. 12 Hii ndiyo sheria kwa
ajili ya nyumba: Kutoka kwenye kilele cha mlima hata mpaka wote unaoizunguka,
patakuwa patakatifu sana. Tazama! Hii ndiyo sheria kwa ajili ya nyumba. 13 Hivi
vitakuwa vipimo vya madhabahu katika dhiraa-hiyo dhiraa kuwa dhiraa ya kawaida
na urefu wa kiganja. Hivyo mfereji ulio uzunguka madhabahu utakuwa dhiraa moja
chini, na upana wake pia utakuwa dhiraa moja. Mpaka wa karibu uizungukayo
machinjio shubiri moja. Hii itakuwa kitako cha madhabahu. 14 Usawa wa kutoka
kwenye mferji hadi kwenye machinijo ya chini ya madhabahu itakuwa dhiraa mbili,
na hiyo machinjio yenyewe itakuwa dhiraa moja upana. Kisha kutoka machinjio
madogo hadi kwenye machinjio makubwa ya madhabahu, itakuwa dhiraa nne, na
machinjio makubwa yatakuwa dhraa moja upana. 15 Meko juu ya madhabahu kwa
ajili ya sadaka ya kuteketezwa ni dhiraa nne juu, na kuna pembe nne zilizoelekea
juu kwenye meku. 16 Meku ina dhiraa kumi na moja urefu na dhiraa kumi na mbili
upana, za mraba. 17 Mpaka wake ni dhiraa kumi na nne urefu na dhiraa kumi na nne
upana pande zake zote nne, na ukingo wake ni nusu dhiraa upana. Mfereji ni dhiraa
moja upana kuzuka kote pamoja na ngazi zielekeazo mashariki." 18 Kisha akanambia,
"Mwanadamu, Bwana Yahwe asema hivi: Hizi ndizo sheria kwa ajili ya madhabahu
katika siku watakayoitengeza, kwa ajili kutoa sadaka ya kuteketezwa kwenye hiyo,
na kwa jili ya kunyunyiza damu juu yake. 19 Utatoa ng'ombe kutoka kwenye kundi
kama sadaka ya dhambi kwa ajili ya Walawi makuhani ambao ni uzao wa Zadoki,
wale wajao karibu nami kunitumikia-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. 20 Kisha
utachukua baadhi ya damu yake na kuiweka juu pembe nne za madhabahu na pande
nne za machinjio na kuuzunguka ukingo; utaitakasa na kufanya upatanisho kwa ajili
yake. 21 Kisha chukua ng'ombe kama sadaka ya dhambi na iteketezwe katika eneneo
lililotengwa la nje ya patakatifu. 22 Kisha katika siku ya pili utatoa mbuzi dume
asiyekuwa na dosari kutoka kundini kama sadaka ya dhambi; makuhani wataisafisha
madhabahu kama walivyoisafisha kwa ng'ombe. 23 Utakapomaliza kusafisha, toa
ng'ombe asiyekuwa na dosari kutoka kwenye mifugo na kondoo dume asiyekuwa na
dosari kutoka kundini. 24 Watoe mbele ya Yahwe; makuhani watanyunyiza chumvi
juu yao na kuwainua juu kama sadaka ya kutekezwa kwa Yahwe. 25 Utaandaa

mbuzi dume kama sadaka ya dhambi kila siku kwa mda wa siku saba, na makuhani
pia wataandaa ng'ombe asiye na dosari kutoka kwenye kundi na kondoo dume
kutoka kwenye kundi. [26] Wataipatanisha madhabahu kwa siku saba na kuitakasa,
wataitakasa kwa njia hii. [27] Watamaliza hizi siku saba, na katika siku ya nane na
kuendelea itakuwa kwamba makuhani wataandaa sadaka za kuteketezwa na sadaka
za amani kwenye madhabahu, ndipo nitakapowakubali-hivi ndivyo Bwana Yahwe
asemavyo."

# 44

[1] Kisha yule mtu akanirudisha hata lango la nje la patakatifu linaloelekea
mashariki; lilikuwa limefungwa kwa kukazwa. [2] Yahwe akanambia, "Hili lango
litakuwa limefungwa; halitafunguliwa. Hakuna mtu atakaye pitia hapo, kwa
kuwa Yahwe, Mungu wa Israeli ameingia kwa hilo, hivyo lilikuwa limefungwa
kwa kukazwa. [3] Mtawala wa Israeli atakaa katika hilo kula chakula mbele ya
Yahwe. Ataingia kwa njia ya varanda na kutoka kwa njia hiyo hiyo." [4] Kisha
akaniletea kwa njia ya lango la kaskazini linaloelekea kwenye nyumba. Hivyo
nikaona na kutazama, utukufu wa Yahwe umejaa kwenye nyumba ya Yahwe,
nikaanguka kifudifudi. [5] Kisha Yahwe akanambia, "Mwanadamu, andaa moyo
wako na tazama kwa macho yako na sikiliza kwa masikio yako kwa yote yale
nikuambiayo, kwa amri zote za nyumba ya Yahwe na maagizo yote. Fikiri kuhusu
malango ya nyumba na na matokeo ya malango. [6] Kisha waambie wale walioasi,
nyumba ya Israeli, 'Bwana Yahwe asema hivi: Acheni matendo yenu maovu
kwenu, nyumba ya Israeli- [7] ambayo mmewaleta wageni pamoja na wasiotahiriwa
mioyo na wasiotahiriwa mwili kuwa katika patakatifu pangu, kuikufuru nyumba
yangu, wakati mlipokuwa mnanitolea chakula, mafuta na damu-mmevunja agano
langu kwa matendo yenu maovu. [8] Hamkumaliza kazi zenu zinazohusiana na
vitu vitakatifu, lakini mmewateua wengine kuchukua kazi zenu, na mmewatuma
kupaangalia mahali patakatifu pangu. [9] Bwana Yahe asema hivi: hakuna mgeni,
ambaye hajatahiriwa kwenye moyo wake na mwili, kutoka yeyote wa hao waishio
miongoni mwa watu wa Israeli, awezaye kuingia patakatifu pangu. [10] Kisha Walawi
wakaenda mbali nami-wakapotea mbali nami, kwenda kwenye sanamu zao-lakini
watalipa kwa ajili ya dhambi yao. [11] Wao ni watumishi katika patakatifu pangu,
waangalizi wa malango ya nyumba na kutumika kwenye nyumba na kuchinja
sadaka za kuteketezwa na dhabihu za watu, na watasimama mbele za watu na
kuwatumikia. [12] Lakini kwa sababu wamefanya dhabihu mbele ya sanamu zao,
wamekuwa kikwazo kwa dhambi ya nyumba ya Israeli. Kwa hiyo nitainua mkono
wangu kuapa kiapo dhidi yao-hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo-watabeba adhabu
yao. [13] Hawatakuja karibu nami kufanya kama makuhani au kukaribiakila vitu
vyangu vitakatifu, vitu vitakatifu sana. Badala yake, watabeba lawama zao na
hatia zao kwa ajili ya matendo yao ya karaha waliyoyafanya. [14] Lakini nitawaweka
kama watunzaji wa kazi katika nyumba, kwa kazi zote na kila kitu kitakachofanyika
ndani yake. [15] Kisha makuhani walawi, hao wana wa Zadoki ambao waliokamilisha
kazi ya patakatifu pangu wakati wana wa Israeli walipotea mbali nami-watakuja
karibu nami kuniambudu. Watasimama mbele yangu kunitolea mafuta na damu-hivi
ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. [16] Watakuja hata patakatifu pangu; wataikaribia
meza yangu kuniabudu na kukamilisha kazi zao kwangu. [17] Hivyo itakuwa kwamba
watakapokuja kwenye malango ya ua wa ndani, watatakiwa kuvaa mavazi ya kitani,
kwa kuwa hawatakuja na sufu ndani ya lango la ua wa ndani na nyumba yake.
[18] Kutakuwa na vilemba juu ya vichwa vyao na kitani ndani ya viuno vyao. Ndani
wasivae nguo ambayo itawafanya watoke jasho. [19] Wakati watakapotoka nje ya

ua wa nje, hata kwenye ua wa ndani ili kwenda kwa watu, watavua nguo zao walizokuwa wamezivaa kisha wakatumika; watazivua na kuziweka chini katika chumba kitakatifu, hivyo wasiwafanye wengine watakatifu kwa kugusana na nguo
zao maalumu. [20] Hawatanyoa vichwa vyao wala kuruhusu nywele zao kuwa ndefu,
watapunguza nywele za vichwa vyao. [21] Hakuna kuhani atakaye ruhusiwa kunywa
mvinyo wakati atakapoingia kwenye uwa wa ndani, [22] hakuna kuchukua mjane au
mwanamke aliyetalikiwa kama mke kwa ajili yake, lakini mwali kutoka safu ya
nyumba ya Israeli au mjane aliyekuwa ameolewa na kuhani aliyepita. [23] Kwa kuwa
watawafundisha watu wangu tofauti kati ya utakatifu na kukufuru; watawafanya
kujua uchafu kutoka usafi. [24] Katika kubishana watasimama kwenye hukumu pamoja
na amri yangu; watakuwa waadilifu. Watashika sheria yangu na amri zangu katika
sikukuu, na watasherekea siku yangu ya Sabato. [25] Hawataenda kwa mtu aliyekufa
ili wasiwe najisi, vinginevyo awe ni baba au mama yao, mwana wa kiume au
binti, kaka au dada ambaye hajawahi kulala na mtu; vinginevyo, watakuwa najisi.
[26] Baada ya kuhani kuwa najisi, watahesabu mda wa siku saba kwa ajili yake.
[27] Katika siku atakayoingia mahali patakatifu, ndani kwenye uzio kutumika katika
mahali patakatifu, ataleta sadaka ya dhambi kwa ajili yake mwenyewe-hivi ndivyo
Bwana Yahwe asemavyo. [28] Hapa patakuwa urithi wao: Mimi ndiyo urithi wao,
na usiwapatie mali katika Israeli; nitakuwa mali yao! [29] Watakula chakula cha
sadaka, sadaka za dhambi, sadaka za hatia, na kila kitakachotolewa kwa ajili ya
Yahwe katika Israeli, vitakuwa vyao. [30] Malimbuko ya kwanza ya vitu na kila sadaka,
kila kitu kitokanacho na sadaka zenu vitakuwa mali ya makuhani, mtatoa sadaka ya
chakula kizuri kwa makuhani ili kwamba baraka iweze kukaa katika nyumba zenu.
[31] Makuhani hawatakula mzoga au mnyama aliyeraruliwa, iwe ni ndege au mnyama.

# 45

[1] Wakati mtakapogawanya nchi kama urithi, mtafanya sadakwa kwa Yahwe;
sadaka hiyo itakuwa sehemu takatifu ya nchi, dhiraa elfu ishirini na tano urefu, na
dhiraa elfu kumi upana. Patakuwa patakatifu, ndani ya mipaka yake yote. [2] Kutoka
hapa kutakuwa na dhiraa mia tano kwa dhiraa mia tano za mraba kuzunguka
mahali patakatifu, kwa kuuzunguka mpaka dhiraa hamsini upana. [3] Kutoka hili
eneo utapima fungu ambalo ni dhiraa elfu ishirini na tano urefu na elfu kumi upana;
patakuwa patakatifu; mahali patakatifu palipo tukuka. [4] Patakuwa patakatifu katika
nchi kwa ajili ya makuhani wanaomtumikia Yahwe, ajaye kwa Yahwe kumtumikia.
Patakuwa mahali kwa ajili ya nyumba na eneo takatifu kwa ajili mahali patakatifu.
[5] Hivyo itakuwa dhiraa elfu ishirini na tano urefu na elfu kumi upana, patakuwa
kwa ajili ya miji ya Walawi wanaotumika kwenye nyumba. [6] Mtadhihirisha eneo
moja kwa ajili ya mji, dhiraa elfu tano na urefu ishirini na tano, hapo patakuwa
kando kando ya eneo lililohifadhiwa kwa ajili ya mahali patakatifu; huu mji utakuwa
wa mali ya nyumba yote ya Israeli. [7] Nchi ya mwana mfalme itakuwa kwa pande
zote za eneo lililohifadhiwa kwa ajili ya mahali patakatifu na mji. Patakuwa kwa
upande wao wa magaharibi na upande wa mashariki. Urefu utalingana na urefu wa
moja ya hayo mafungu, kutoka magaribi hata mashariki. [8] Hii nchi itakuwa mali ya
mwana mfalme katika Isaraeli. Wana wafalme hawatawakandamiza watu wangu;
badala yake, watawapatia nchi kwa nyumba ya Israeli, kwa ajili ya makabila yao.
[9] Bwana Yahwe asema hivi: Inatosha kwa ajili yenu, mwana mfalme wa Israeli!
Ondoa dhuluma na mgogoro; fanya hukumu na haki! Usiwafukuze wapangaji wa
watu wangu! -hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. [10] Mtakuwa na mzani sahihi,
efa sahihi, na bathi sahihi! [11] Efa na bathi zitakuwa kiasi kile kile, ili kwamba
bathi iwe zaka ya homeri; efa itakuwa zaka ya hamori moja. Vipimo vyao vitakuwa

vinafanana na homeri. [12] Shekeli zitakuwa gera ishirini, shekeli sita zitakuwa mane
yenu. [13] Hili ndilo toleo mtakalotoa: efa sita kwa kila homeri ya ngano, na mtatoa
efa sita kwa kila homeri ya shayiri. [14] Sadaka ya kawaida ya mafuta itakuwa zaka ya
bathi kwa kila kori (ambazo ni bathi), au kwa kila hamori, kwa kuwa hamori moja
ni bathi kumi pia. [15] Kondoo mmoja au mbuzi kutoka mifugo kwa kila wanyama
mia mbili kutoka malisho ya maji ya mikoa ya Israeli yatatumika kwa sadaka ya
kuteketezwa yoyote au sadaka ya amani kufanya upatanisho kwa ajili ya watu-hivi
ndivyo Bwana Yahwe asemavyo. [16] Watu wote wa nchi watatoa hii sadaka kwa
mwana mfalme wa Israeli. [17] Utakuwa wajibu wa mwana mfalme kutoa wanyama
kwa ajili ya sadaka za kuteketezwa, sadaka ya unga, sadaka ya kinywaji, katika siku
za sikukuu na sherehe za mwezi mpya, na katika siku za Sabato-sikukuu zote za
kudumu za nyumba ya Israeli. Ataandaa kwa ajili ya sadaka za dhambi, sadaka za
unga, sadaka za kuteketezwa, na sadaka za amani kwa ajili ya upatanisho badala ya
nyumba ya Israeli. [18] Bwana Yahwe asema hivi: Katika mwezi wa kwanza, siku ya
kwanza ya mwezi, utachukua ng'ombe mmoja asiyekuwa na dosari kutoka kwenye
kundi na kufanya sadaka ya dhambi kwa ajili ya patakatifu. [19] Kuhani atachukua
baadhi ya damu ya sadaka ya dhambi na kuiweka juu ya miimo ya mlango na
kwenye pembe nne za mpaka wa madhabahu, na miimo ya lango la uzio wa ndani.
[20] Utafanya hivyo siku ya saba ya mwezi kwa dhambi ya kila mtu kwa ajali au ujinga;
katika njia hii mtaipatanisha hekalu. [21] Katika siku ya mwezi siku ya kumi na nne
ya mwezi, mtakuwa na sikukuu, sikukuu ya siku saba. Matakula makate usiotiwa
chachu. [22] Siku hiyo, mwana mfalme ataandaa ng'ombe kwa ajili yake na kwa ajili
ya watu wote wa nchi kama sadaka ya dhambi. [23] Kwa siku saba za sikukuu, mwana
wa mfalme ataandaa sadaka ya kuteketezwa kwa ajili ya Yahwe: ng'ombe saba na
kondoo dume saba zisizokuwa na dosari kila siku kwa mda wa siku saba, na mbuzi
dume kila siku kama sadaka ya dhambi. [24] Kisha mwana mfalme atatengeneza
sadaka ya chakula ya efa moja kwa kila ng'ombe na efa moja kwa kila kondoo dume
pamoja na hini ya mafuta kwa kila efa. [25] Katika siku ya saba ya mwezi siku ya kumi
na tano ya mwezi, katika sikukuu, mwana wa mfalme atafanya matoleo katika siku
hizi saba: sadaka za dhambi, sadaka za kuteketezwa, sadaka za chakula, na sadaka
za mafuta.

# 46

[1] Bwana Yahwe asema hivi: Lango la uzio wa ndani, linaloelekea mashariki,
litafungwa kwa mda wa siku sita za kazi, lakini katika siku za Sabato litakuwa wazi,
na katika siku ya mwezi mpya litafunguliwa. [2] Mwana wa mfalme ataingia kwa
kutumia lango la njia ya nyuma ya varanda upande wa nje, na atasimama mbele
ya muhimili wa mwimo wa lango la ndani wakati makuhani wakiwa wakitengeza
sadaka ya kuteketezwa na sadaka ya amani. Kisha ataabudu kwenye kizingiti cha
lango la ndani na kutoka nje, lakini lango halitakuwa linafungwa hadi jioni. [3] Watu
wa nchi pia wataabudu mbele ya Yahwe kwenye hili lango la kuingilia katika siku ya
Sabato na siku mpya za mwezi. [4] Sadaka ya kuteketezwa ambayo mwana wa mfalme
aitoayo kwa Yahwe katika siku ya Sabato itakuwa wanakondoo sita wasiokuwa
na dosari na kondoo dume asiyekuwa na dosari. [5] Sadaka ya unga pamoja na
kondoo dume itakuwa efa moja, na sadaka ya unga pamoja na wanakondoo kiasi
awezacho kutoa, na hini moja ya mafuta pamoja na kila efa ya unga. [6] Katika siku
ya mwezi mpya atatoa ng'ombe mchanga asiyekuwa na dosari kutoka kuchungwa,
wanakondoo sita, na kondoo asyekuwa na dosari. [7] Atatengeneza sadaka ya unga
ya efa moja kwa ajili ya ng'ombe na efa moja kwa ajili ya kondoo, na kwa kiasi
awezacho kukitoa kwa ajili ya wanakondoo, na hini ya mafuta kwa kila efa ya

unga. 8 Wakati mwana wa mfalme atakapokuwa anaingia kwa njia ya lango lenye
varanda, ataondoka kwa njia hiyo hiyo. 9 Lakini wakati watu wa nchi watakakuja
kwa Yahwe katika sikukuu zilizoteuliwa, kila mmoja kuingia kupitia kwenye lango la
kaskazini kuabudu ataondoka kupitia lango la kusini; na kila atakayeingillia kupitia
lango la kusini atatoka kupitia lango la kaskazini. Hakuna atakayerudia kwa lile
lango aliloingilia, kwa kuwa atatoka nje moja kwa moja. 10 Mwana wa mfalme
atakuwa kati yao; watakapoingia, ataingia ndani, na watakapoondoka, atatoka nao.
11 Kwenye sikukuu hizo, sadaka ya unga itakuwa efa moja ya unga kwa ng'ombe
mmoja na efa moja kwa kondoo dume, na chochote atakacho kitoa pamoja na
wanakondoo, na hini moja ya mafuta kwa kila efa. 12 Wakati mwana wa mfalme
atakapotoa sadaka atakayojisikia kutoa, labda sadaka ya kuteketezwa au sadaka ya
amani kwa Yahwe, lango la kuelekea mashariki litafunguliwa kwa ajili yake. Atatoa
sadaka yake ya kuteketezwa au sadaka ya amani kama afanyavyo siku ya Sabato.
Kisha atatoka nje, na baada ya kutoka lango litafungwa. 13 Kwa kuongeza, utatoa
mwanakondoo asiyekuwa na dosari mwenye umri wa mwaka mmoja kama sadaka
ya kuteketezwa kwa Yahwe kila siku; utafanya hivi kila asubuhi. 14 Utatoa sadaka
ya unga pamoja nayo kila asubuhi, efa sita na sehemu ya tatu ya hini ya mafuta
kuchanganya na sadaka ya unga kwa ajili ya Yahwe, kulingana na sheria ilivyo.
15 Watandaa mwanakondoo, sadaka ya kuteketezwa, na mafuta kila asubuhi, sadaka
ya kuteketezwa ya kudumu. 16 Bwana Yahwe asema hivi: Kama mwana wa mfalme
akitoa zawadi kwa mmoja wa watoto wake, imekuwa urithi wake. Itakuwa mali ya
mtoto wake, imekuwa urithi. 17 Lakini kama akimpatia zawadi kutoka urithi wake
kwa mmoja wa watumishi wake, kisha itakuwa ya huyo mtumishi mpaka mwaka wa
uhuru, na kisha itarudi kwa mwana wa mfalme. Urithi wake yamkini ukawa kwa
ajili ya watoto wake. 18 Mwana wa mfalme hatawaondolea urithi wa watu kutoka
kwenye mali zao wenyewe; ataandaa kwa ajili ya watoto wake mali ili kwamba watu
wangu wasitawanyike, kila mtu kutoka mali kwenye yake mwenyewe." 19 Kisha yule
mtu akaniletea kwenye lango la kutokea hata kwenye vyumba vitakatifu kwa ajili ya
makuhani, vilivyokuwa vimeelekea kaskazini na tazama! Kulikuwa na sehemu mbele
magharibi. 20 Akanambia, "Hii ndio sehemu ambayo makuhani watakapo chemshia
sadaka ya hatia na sadaka ya dhambi na walipookea sadaka ya unga. Wasilete sadaka
nje ya uzio, kwa kuwa watu watatakaswa." 21 Kisha akanileta kwenye uzio wa nje
akaniongoza kuzunguka pembe nne za uzio, nikaona kwamba katika kila pembe ya
uzio kulikuwa na uwanja. 22 Katika hizo pembe nne za nje ya uzio kulikuwa na nzio
nne ndogo, dhiraa arobaini urefu na thelathini upana. Ukubwa ule ule kwa nzio zote
nne. 23 Kulikuwa na safu zilizokuwa zimetengenezwa kwa mawe kuzizunguka zote
nne, na meko ya kupikia ilikuwa chini ya safu ya jiwe. 24 Yule mtu akanambia, "Hizi
ndizo sehemu ambazo watumishi watachemshia dhabihu za watu."

# 47

1 Kisha yule mtu akanirudisha nyuma kwenye lango la kuingia la hekalu, na
kulikuwa na maji yakitiririka nje kutoka chini ya hekalu kizingiti cha nyumba
kuelekea masharikii-kwa mbele ya hekalu kulekea mashariki-na maji yalikuwa
yakitiririka chini upande wa kusini mwa hekalu, kuelekea upande wa kuume wa
madhabahu. 2 Hivyo akanileta kwenye lango la kaskazini na kuniongoza kuzunguka
lango kuelekea mashariki, na hapo maji yalikuwa yakitiririka kutoka lango hili kwa
upande wa kusini yake. 3 Yule mtu alipokuwa akienda mashariki, kulikuwa na kamba
ya kupimia kwenye mkono wake; akapima dhiraa elfu moja akanivusha kwenye maji
hata maji yakafika kwenye magoti. 4 Kisha akapima dhiraa elfu moja ten akanivusha
kwenye yale maji yaliyofika kwenye magoti; akapima dhiraa elfu kumi nyingine na

kunivusha maji yakafika hata kwenye nyonga. 5 Tena akapima dhiraa elfu moja
nyingine, lakini ulikuwa mto ambao sikuweza kuuvuka kwa sababu maji yalizidi
na yalijaa maji ya kuogelea ndani-yalikuwa mto usiovukika 6 Yule mtu akanambia,
“Mwanadamu, unaona hii?” akanipeleka na kunirudisha karibu na ukingo wa mto.
7 Nilipokuwa nikirudi, hapo kwenye ukingo wa mto kulikuwa na miti mingi katika
huu upande na upande mwingine pia. 8 Yule mtu akanambia, “Haya maji yanatoka
kwenda pande za nchi ya mashariki na chini hata Araba; haya maji hutiririka
kwenye Bahari ya Chumvi itaifanya kuwa mpya. 9 Itakuwa kwamba kila kiumbe
hai kisongamanacho kitaishi mahali maji yanapoelekea; kutakuwa na samaki wengi,
kwenye hayo maji yatiririkayo huko. Itafanya maji ya chumvi kuwa mapya. Kila
kitu kitaishi popote mto utakapoelekea. 10 Kisha itatokea kwamba wavuvi wa En
Gedi watasimama karibu na maji, na kutakuwa na sehemu ya kutandazia nyavu za
samaki karibu na En Eglaimu. Kutakuwa na samaki nyingi za aina tofauti tofauti
katika Bahari ya Chumvi, kama samaki kwenye Bahari Kuu kwa wingi wao. 11 Lakini
Bahari ya Chumvi ikajaa maji na matope hayataachwa mapya; yataachwa yawe kwa
ajili ya kutengeneza chumvi. 12 Karibu na huo mto juu ya ukingo wake, pande
zote, aina zote za miti utazaa chakula. Majani yake hayatanyauka na matunda
yake hayataacha kukua. Kila mwezi miti itazaa matunda, kwa sababu maji kutoka
patakatifu yatatirirka kwenda kwenye hiyo miti. Matunda yake yatakuwa kwa ajili
ya chakula, na majani yake yatakuwa kwa ajili ya dawa. 13 Bwana Yahwe asema
hivi: Hii itakuwa njia ambayo mtaigawanya nchi kwa ajili ya kabila kumi na mbili
za Israeli: Yusufu atakuwa na mafungu mawili. 14 Mtaigawa kila mtu sawa sawa
ambayo niliinua mkono wangu na kuapa kuwapa baba zenu. Hii nchi itakuja kuwa
urithi kwenu. 15 Huu utakuwa mpaka wa nchi upande wa kaskazini kutoka Bahari
Kubwa kwa njia ya Hethloni, na kisha kuelekea Zedada. 16 Kisha mpaka utaenda
hata Berotha, hadi Sibraimu, iliyopo kati ya Damaskasi na Hamathi, na kisha hata
Hazer-hatikoni, iliyopo karibu na mpaka wa Haurani. 17 Hivyo mpaka utaenda kutoka
kwenye bahari hadi Hazar-enoni kwenye mpaka wa Damaskasi na Hamathi hata
kaskazini. Huu utakuwa upande wa kaskazini. 18 Kwa upande wa mashariki, kati ya
Haurani na Damaskasi na kati ya Geliadi na nchi ya Israeli kutakuwa na mto Yordani.
Mtapima kutoka kwenye mpaka hata kwenye bahari ya mashariki; huo wote utakuwa
mpaka wa mashariki. 19 Kisha upande wa kusini: kusini mwa Tamari hadi kwenye
maji ya Meriba Kadeshi, kijito cha Misri hata Bahari Kuu, na upande wa kusini
kuelekea kusini. 20 Kisha mpaka wa magharibi utakuwa Bahari Kuu utaelekea hata
nyuma ya Hamathi. Huu utakuwa upande wa mgharibi. 21 Kwa njia hii mtaigawanya
hii nchi kwa ajili yenu wenyewe, kwa kabila za Israeli. 22 Hivyo mtagawana urithi
kwa ajili yenu wenyewe na kwa ajili ya wageni walio kati yenu, wale watakaozaa
watoto kati yenu na waliokuwa, kati yenu, kama wazaliwa wa watu wa Israeli.
Mtapewa urithi miongoni mwa makabila ya Israeli. 23 Kisha itatokea kwamba wageni
watakuwa pamoja na kabila miongoni mwa yule anayeishi. Mtapatia urithi-hivi
ndivyo Bwana Yahwe asemavyo.”

# 48

1 Haya ndiyo majina ya makabila. Kabila la Dani litapokea sehemu moja ya nchi;
mipaka yake itakuwa karibu na upande wa mashariki mpaka wa Israeli karibu na
njia ya Hethloni na Lebo Hamathi. Mpaka wake utaenda hata karibu na Hazari
Enani na karibu na mpaka wa Damaskasi hata upande wa kaskazini na kisha karibu
na Hamathi. Mpaka wa Dani utaenda kutoka mashariki moja kwa moja hata Bahari
Kubwa. 2 Kupakana na mpaka wa Dani, kutoka upande wa mashariki hata upande wa
magharibi, Asheri itakuwa na fungu moja. 3 Kupakana na mpaka wa Asheri kutoka

upande wa mashariki hata magharibi, Naftali atakuwa na fungu moja. 4 Kupakana
na mpaka wa Naftali kutoka upande wa mashariki hata magharibi, Manase atakuwa
na fungu moja. 5 Kupakana na mpaka wa Manase kutoka upande wa mashariki hata
magharibi, Efraimu atakuwa na fungu moja. 6 Kupakana na mapaka wa Efraimu
kutoka mashariki hata magharibi, Rubeni atakuwa na fungu moja. 7 Kupakana na
mpaka wa Rubeni kutoka mashariki hata magharibi, Yuda atakuwa na fungu moja.
8 Sadaka ya nchi ambayo mtaifanya itakuwa karibu na mpaka wa Yuda na hapohapo
kutoka upande wa mashariki hata upande wa magharibi; itakuwa ridhaa elfu ishirini
na tano upana. Urefu unakaribiana na fungu la kabila moja kutoka upande wa
mashariki hata upande wa magharibi, na hekalu litakuwa katikati yake. 9 Huu mji
mtakao utoa sadaka kwa ajili ya Yahwe utakuwa na ridhaa elfu ishirini na tano
urefu wake na ridhaa elfu kumi upana. 10 Haya yatakuwa matoleo ya hili fungu
takatifu la nchi: makuhani watakuwa na nchi watakayopewa kipimo chake ridhaa
elfu ishirini na tano urefu kwa upande kaskazini; ridhaa elfu kumi upana upande
wa magharibi; urefu wa ridhaa elfu kumi upande wa magharibi; na urefu rithaa elfu
ishirini na tano upande wa kusini, pamoja na mahali patakatifu pa Yahwe katikati
yake. 11 Hii itakuwa wakfu na makuhani wa safu ya Zadoki, aliyenitumikia kwa
uaminifu na ambaye hakwenda nje ya mstari wakati watu wa Israeli walipoeenda
nje ya mstari, kama Walawi walivyofanya. 12 Sadaka yao itakuwa fungu la hiyo nchi
takatifu sana, karibu na mpaka wa Walawi. 13 Nchi ya Walawi karibu na mpaka wa
nchi ya makuhani itakuwa ridhaa elfu ishirini na tano urefu na ridhaa elfu kumi
upana. Urefu wote wa eneo la nchi utakuwa ridhaa elfu ishirini na tano urefu
na ridhaa elfu ishirini upana. 14 Hawataiuza au kuibadilisha; hakuna malimbuko
ya hiyo nchi ya Israeli itakayogawanywa kutoka haya maeneo, kwa kuwa yote ni
matakatifu kwa ajili ya Yahwe. 15 Nchi iliyobaki, ridhaa elfu kumi na tano upana
na ridhaa elfu ishirini na tano urefu, itakuwa kwa wote wanayoitumia hiyo nchi,
nyumba, na sehemu ya malisho; huo mji utakuwa katikati yake. 16 Hivi ndivyo
vitakuwa vipimo vya mji: upande wa kaskazini utakuwa ridhaa 4, 500 urefu; upande
wa kusini utakuwa ridhaa 4, 500 urefu; upande wa magharibi utakuwa ridhaa 4,
500 urefu; na magharibi itakuwa ridhaa 4, 500 urefu. 17 Kutakuwa na malisho ya
mji kuelekea kaskazini, ridhaa 250 kwenda chini; hata kusini, ridhaa 250 kwenda
chini; kuelekea mashariki, ridhaa 250 kwenda chini, na kuelekea magharibi ridhaa
250 kwenda chini. 18 Eneo lililobaki la matoleo matakatifu litanyooshwa ridhaa elfu
kumi hata mashariki na ridhaa elfu kumi kuelekea magharibi. Litanyooshwa karibu
na mpaka wa matoleo matakatifu, na mazao yake yatakuwa chakula kwa ajili ya
wale wanaofanya kazi katika nchi. 19 Wale wafanyao kazi katika mji, watu wote wa
kabila za Israeli, watailima hiyo nchi. 20 Matoleo yote ya nchi yatapimwa ridhaa elfu
ishirini na moja kwa ridhaa elfu ishirini na tano. Kwa njia hii mtatengeneza matoleo
matakatifu ya nchi, pamoja na nchi kwa ajili mji. 21 Mabaki ya nchi mojawapo
upande wa matoleo matakatifu na eneo la mji litakuwa kwa ajili ya mwana wa
mfalme. Eneo la nchi ya mwana wa mfalme kuelekea mashariki litanyooshwa kwa
ridhaa elfu ishirini na tano kutoka kwenye mpaka wa matoleo matakatifu hata
mpaka wa mashariki-na eneo lake kuelekea mpaka wa magharibi. Katikati kutakuwa
matolea matakatifu, na mahali patakatifu pa hekalu patakuwa katikati yake. 22 Nchi
imenyooka kutoka mali ya Walawi na eneo la mji katikati yake litakuwa kwa ajili ya
mwana wa mfalme; itakuwa kati ya mpaka wa Yuda na mpaka wa Benjamini-hiyo
nchi itakuwa kwa ajili ya mwana wa mfame. 23 Kwa kabila zitakazobaki, mafungu
yao yataunganishwa kutoka upande wa mashariki. Benjamini atapokea fungu moja.
24 Kupakana na mpaka wa Benjamini kutoka upande wa mashariki hata magharibi,
Simioni atakuwa na fungu moja. 25 Kupakana na mpaka wa Isakari kutakuwa na

fungu moja. 26 Kupakana na mpaka wa Isakari kutoka mashariki hata magharibi,
Zebuloni atakuwa na fungu moja. 27 Hata kusini mwa mpaka wa Zebuloni, kutoka
upande wa mashariki hata upande wa magahribi, kutakuwa na nchi ya Gadi-fungu
moja. 28 Mpaka wa kusini mwa Gadi kutanyooshwa kutoka Tamari hata kwenye maji
ya Meriba Kadeshi, mbele hadi kijito cha Misri, na kisha hata Bahari kuu. 29 Hii
ndiyo nchi ambayo mtakazo gawana; kutakuwa na urithi wa makabila ya Israeli.
Haya yatakuwa mafungu yao. Hivi ndivy Bwana Yahwe asemavyo. 30 Hawa ndio
watakaoishi kutoka kwenye nchi: upande wa kaskazini, ambapo patapimwa ridhaa
4, 500 kwa urefu, 31 kutakuwa na malango matatu, yaitwayo kwa ajili ya Israeli: lango
moja kwa ajili ya Rubeni, lango moja kwa ajili ya Yuda, na lango moja kwa ajili ya
Walawi. 32 Kwa upande wa mashariki, ambapo patapimwa ridhaa 4, 500 kwa urefu,
kutakuwa na malango matatu: lango moja kwa ajili ya Yusufu, lango moja kwa ajili ya
Benjamini, na lango moja kwa ajili ya Dani. 33 Kwa upande wa mashariki, kutakuwa
na kipimo cha ridhaa 4, 500 urefu, kutakuwa na malango matatu: lango moja kwa
ajili ya Simioni, lango moja kwa ajili ya Isakari, na moja kwa ajili ya Zebuloni. 34 Kwa
upande wa magharibi, ambao kipimo chake kitakuwa ridhaa 4, 500, kutakuwa ba
malango matatu: lango moja kwa ajili ya Gadi, lango moja kwa ajili ya Asheri, na
lango moja kwa ajili ya Naftali. 35 Umbali kuuzunguka mji utakuwa ridhaa elfu kumi
na nane; kutoka hiyo siku, jina la huo mji litakuwa “Yahwe yupo hapo.”

# Danieli

[1] Katika mwaka wa tatu wa utawala wa Yehoyakimu mfalme wa Yuda, Nebukad-
neza mfalme wa Babeli alikuja Yerusalemu na kuuzunguka mji ili kuzuia mahitaji
yake yote. [2] Bwana alimpa Nebukadneza ushindi dhidi ya Yehoyakimu mfalme
wa Yuda, na alimpatia vitu vitakatifu kutoka nyumba ya Mungu. Alivipeleka vitu
hivyo mpaka katika nchi ya Babeli, kwa nyumba ya mungu wake, na aliviweka
vitu vitakatifu katika hazina ya mungu wake. [3] Mfalme akamwambia Ashipenazi,
afisa wake mkuu, awalete baadhi ya watu wa Israeli, wa familia ya kifalme na za
kiungwana - [4] vijana wasio na hila, wenye mwonekano wa kuvutia, wenye ujuzi
katika hekima yote, wenye kujawa na ufahamu na weledi, na wenye sifa za kutumika
katika ikulu ya mfalme. Alitakiwa kuwafundisha maandiko na lugha ya Babeli.
[5] Mfalme aliwatengea kwa ajili yao fungu kutoka katika chakula chake kizuri kwa
kila siku na katika divai aliyokunywa. Vijana hawa walitakiwa kufunzwa kwa
miaka mitatu, na baada ya hapo, wangeweza kumtumikia mfalme. [6] Miongoni mwao
walikuwa ni Danieli, Hanania, Mishaeli, na Azaria, baadhi ya watu wa Yuda. [7] Afisa
mkuu aliwapa majina: Danieli alimwita Belteshaza, Hanania alimwita Shadraka,
Mishaeli alimwita Meshaki, na Azaria alimwita Abedinego. [8] Lakini Danieli alinuia
katika akili yake kuwa asingejitia ujanisi mwenyewe kwa chakula kizuri cha mfalme
wala kwa divai ambayo alikunywa. [9] Basi, aliomba ruhusa kutoka kwa afisa mkuu
ili kwamba asije akajitia uchafu yeye mwenyewe. Hivyo, Mungu alimpa Danieli
kibali na huruma kupitia katika heshima ambayo afisa mkuu alikuwa nayo kwake.
[10] Afisa mkuu alimwambia Danieli, “Ninamwogopa bwana wangu mfalme. Ameagiza
aina ya chakula na vinywaji mnavyotakiwa kutumia. Kwa nini awaone ninyi
mkiwa mnaonekana vibaya kuliko vijana wengine wa umri wenu? Mfalme aweza
kukitwaa kichwa changu kwa sababu yenu. [11] Kisha Daniel akamwambia msimamizi
ambaye afisa mkuu alikuwa amemweka juu ya Danieli, Hanania, Mishaeli, na Azaria.
[12] Alisema, “Tafadhari tujaribuni, sisi watumishi wako kwa siku kumi. Tupatieni tu
mboga mboga za kula na maji ya kunywa. [13] Kisha ulinganishe mwonekano wetu na
mwonekano wa vijana wanaokula vyakula vya mfalme, na mtutendee, sisi watu wako
kulingana na kile unachokiona.”' [14] Hivyo msimamizi alikubaliana naye kufanya
hivi, na aliwajaribu kwa siku kumi. [15] Katika mwisho wa siku kumi mwonekano
wao ulikuwa ni wenye afya nzuri kuliko wa wale vijana waliokula vyakula vya
kifalme. [16] Basi, msimamizi aliliondoa fungu lao la chakula na vivywaji vyao na
walipewa mboga mboga tu. [17] Na kuhusu vijana hawa nne Mungu aliwapa uelewa na
ufahamu katika maandiko yote na hekima, na Danieli aliweza kupambanua aina zote
za maono na ndoto. [18] Katika mwisho wa muda uliokuwa umepangwa na mfalme
kuwaleta ndani, afisa mkuu aliwaleta mbele ya Nebukadneza. [19] Mfalme aliongea
nao, na miongoni mwa kundi lote hapo hapakuwa na wa kuwalinganisha na akina
Danieli, Hanania, Mishaeli, na Azaria. Walisimama mbele ya mfalme, wakiwa tayari
kumtumikia. [20] Katika kila swali la hekima na ufahamu ambalo mfalme aliwauliza,
aliwakuta wakiwa na uwezo mara kumi kuliko waganga wote na wale waliojidai
kusema na wafu, waliokuwa katika ufalme wake wote. [21] Danieli alikuwa hapo
mpaka mwaka wa kwanza wa Mfalme Koreshi.

## 2

[1] Katika mwaka wa pili wa utawala wa Nebukadneza, alikuwa na ndoto. Akili yake
ilisumbuka, na hakuweza kulala. [2] Ndipo mfalme alipowaita waganga na wale wenye

kuongea na wafu. Lakini pia aliwaita wachawi na watu wenye hekima. Aliwataka
wamwambie juu ya ndoto zake. Basi walikuja na kusimama mbele za mfalme.
3 Mfalme akawambia, “Nilikuwa na ndoto, na akili yangu ina mashaka nataka kujua
ndoto hiyo nini maana yake.” 4 Kisha watu wenye hekima wakamwambia mfalme
katika Kiaramaiki, “ Mfalme, aishi milele! Twambie sisi ndoto, watumishi wako,
nasi tutaifunua maana yake.” 5 Mfalme akawajibu watu wenye hekima, “ Jambo
hili limeshamalizika. Kama hamtaweza kuiweka wazi ndoto kwangu na kuitafsiri,
miili yenu itakatwa vipande vipande na nyumba zenu zitafanywa kuwa vichuguu
vya uchafu. 6 Lakini kama mtaniambia ndoto na maana yake, mtapokea zawadi
kutoka kwangu, thawabu, na heshima kubwa. Basi niambie ndoto na maana yake.”
7 Wakamjibu tena na kusema, “Mfalme na atuambie, watumishi wake, ndoto nasi
tukwambia maana yake.” 8 Mfalme akawajibu, “ Ninajua kwa hakika mnahitaji
muda zaidi kwasababu mmeona maamuzi yangu ni magumu kuhusu jambo hili.
9 Lakini kama hamtaweza kuniambia ndoto, kuna sentensi moja tu kwa ajili yenu.
Mmeamua kuandaa uongo na maneno ya kudanganya ambayo mmekubaliana kwa
pamoja kuniambia mpaka pale nitakapobadili akili zangu. Basi, niambieni ndoto,
na kisha nitajua kuwa mnaweza kuitafsiri kwa ajili yangu.” 10 Watu wenye hekima
wakamjibu mfalme, “ Hakuna mtu katika dunia anayeweza kutimiza matakwa ya
mfalme. Hakuna mfalme yoyote mkuu na mwenye nguvu ambaye alishataka jambo
kama hilo kutoka kwa wachawi, wala wenye kuongea na wafu, wala mwenye hekima.
11 Kile anachokitaka mfalme ni kigumu, na hakuna yeyote awezaye kumwambia
mfalme isipokuwa miungu, ambayo haishi miongoni mwa watu.” 12 Jambo hili
lilimfanya mfalme akasirike na kughadhabika sana, na alitoa amri kuwaangamiza
wale wote waliojulikana kuwa ni wenye hekima zao katika Babeli. 13 Hivyo, amri
ilitoka kwamba wale wote waliojulikana kwa hekima yao ni lazima wauawe. Na
kwa sababu ya amri hii, walimtafuta Daniel na rafiki zake ili kwamba wauawe.
14 Ndipo Daniel alipomjibu kwa busara na umakini, Arioki, kamanda wa walinzi
wa mfalme, ambaye alikuwa amekuja kuwaua wale wote waliojulikana kuwa na
hekima katika Babeli. 15 Danieli alimwuliza kamanda wa mfalme, “ Kwanini amri ya
mfalme ni ya haraka hivyo?” Hivyo, Arioki akamwambia Danieli kile kilichotokea.
16 Ndipo Danieli aliingia ndani na akaomba ahadi ya muda wa kuonana na mfalme
ili kwamba aweze kuwasilisha tafsiri kwa mfalme. 17 Kisha Danieli aliingia ndani ya
nyumba na aliwaelezea Hanania, Mishaeli, na Azaria, kile kilichotokea. 18 Aliwasihi
kutafuta rehema kutoka kwa Mungu wa mbinguni kuhusiana na siri hii ili kwamba
yeye na wao wasije wakauawa pamoja na watu wengine waliosalia waliojulikana
kuwa na hekima katika Babeli. 19 Usiku ule siri ilifunuliwa kwa Danieli katika
maono. Kisha Danieli akamtukuza Mungu wa mbinguni 20 na kusema, “Litukuzwa
jina la Mungu milele na milele; kwa kuwa hekima na nguvu ni zake. 21 Anabadili
wakati na majira; anaondoa wafalme na kuweka wafalme katika viti vyao vya
enzi. Anawapa hekima wenye hekima na ufahamu kwa wenye weledi. 22 Hufunua
vitu vya chini na vilifichika kwa sababu anajua kile kilicho gizani, naye anaishi
pamoja na mwanga. 23 Mungu wa baba zetu, ninakushukuru na kukutukuza wewe
kwa ajili ya hekima na nguvu uliyonipa. Sasa umeyafanya yawe wazi kwetu
yale tuliyokuomba; umetujulisha mambo yamhusuyo mfalme.” 24 Ndipo Danieli
alienda kumwona Arioki ( yule ambaye mfalme alimchagua kuua kila mtu aliyekuwa
na hekima katika Babeli). Alimwendea na kumwambia, “Usiwauwe watu wenye
hekima katika Babeli. Nipeleke kwa mfalme na nitamwonesha mfalme tafsiri
ya ndoto yake.” 25 Kisha Arioki kwa haraka alimleta Danieli mbele za mfalme
na kusema, “ Nimempata miongoni wa watu wa mateka wa Yuda mtu ambaye
atafunua maana ya ndoto ya mfalme.” 26 Mfalme akamwambia Danieli (ambaye

alikuwa akiitwa Beliteshaza), “Je unaweza kunimbia ndoto niliyoiona na maana
yake?” 27 Danieli alimjibu mfalme na kusema, “Siri ambayo mfalme ameiomba
haiwezi kufunuliwa na watu wenye hekima, wala wale wenye kuongea na wafu,
wala wachawi, na wala wataalamu wa nyota. 28 Isipokuwa kuna Mungu ambaye
anaishi mbinguni, ambaye hufunua siri, na amekwisha kukujulisha wewe, mfalme
Nebukadneza, kile kitakachotokea katika siku zijazo. Hizi ndizo Ndoto na maono
ya akili zako uliyoyaona wakati ulipokuwa umelala kitandani mwako. 29 Na kwako
Wewe, mfalme, mawazo yako kitandani mwako yalikuwa ni juu ya mambo yajayo,
na yule afichuaye siri ameifanya ijulikane kwako kuhusu kile kilicho karibu kutokea.
30 Na kuhusu mimi, siri hii haikufunuliwa kwangu kwa sababu ya hekima yoyote
niliyo nayo zaidi ya mtu yoyote anayeishi. Siri hii imefunliwa kwangu ili kwamba
wewe, mfalme, uweze kufahamu maana, na ili kwamba ujuwe mawazo yaliyo ndani
mwako. 31 Mfalme, uliangalia juu na ukaona sanamu kubwa. Sanamu hii ambayo
ilikuwa yenye nguvu na yenye kung'aa, ilisimama mbele yako. Mng'ao wake ulikuwa
unatisha. 32 Kichwa cha sanamu kilikuwa kimetengenezwa kwa dhahabu safi. Matiti
yake na mikono ilikuwa ya fedha. Sehemu ya katikati na mapaja yake yalikuwa
yametengenezwa kwa shaba, 33 na miguu yake ilikuwa imetengenezwa kwa chuma.
Miguu yake ilikuwa ilitengenezwa kwa sehemu chuma na sehemu kwa udongo.
34 Ulitazama juu, na jiwe lilikuwa limechongwa, ingawa si kwa mikono ya wanadamu,
na liliipiga sanamu katika miguu yake ya chuma na udongo, na ponda ponda.
35 Kisha chuma, udongo, fedha, na dhahabu zilivunjwa katika vipande vipande kwa
wakati mmoja na yakawa kama makapi yaliyo katika sakafu za kupuria kipindi
cha kiangazi. Upepo huyapeperushia mbali na hakuna alama inayoachwa. Lakini
jiwe lililoipiga sanammu likawa mlima mkubwa na kuijaza dunia yote. 36 Hii ndiyo
ilikuwa ndotoyako. Na sasa tutamwambia mfalme maana yake. 37 Wewe, mfalme,
ni mfalme wa wafalme kwa wale ambao Mungu wa mbinguni amekupa ufalme,
nguvu, uweza na heshima. 38 Amevitia mkononi mwako sehemu ambazo binadamu
huishi. Amekupa wanyama wa mwituni na ndege wa angani katika mkono wako,
na amekufanya wewe utawale juu yao wote. Wewe u kichwa cha dhahabu cha
sanamu. 39 Baada yako, ufalme mwingine utainuka ambao ni mdogo kwako, na hata
ufalme wa tatu wa shaba utatawala juu ya dunia yote. 40 Kutakuwa na ufalme wa
tatu, wenye nguvu kama chuma, kwa kuwa chuma huvunja vipande vipande vitu
vingine na kuponda ponda kila kitu. Itaviharibu vitu hivi vyote na kuvisaga. 41 Kama
vile ulivyoona, miguu na vidole vilikuwa kwa sehemu vimetengenezwa kwa udongo
na kwa sehemu vimefanywa kwa chuma, hivyo utakuwa ni ufalme uliogawanyika;
baadhi ya nguvu za chuma zitakuwa ndani yake, kama tu ulivyoona kuwa chuma
kimechanganyikana na udongo laini. 42 Kama vile vidole vya miguuni vilivyokuwa
kwa sehemu vimetengenezwa kwa chuma na kwa sehemu vimetengenezwa kwa
udongo, ndivyo ufalme utakuwa kwa sehemu una nguvu na kwa sehemu utakuwa
dhaifu. 43 Kama ulivyoona chuma kimechanganywa na udongo laini, na hivyo
na watu watakuwa wamechanganyikana; hawakaa kwa pamoja, kama vile chuma
kisivyoweza kushikamana na udongo 44 Katika siku za wafalme hao, Mungu wa
mbinguni ataanzisha ufalme ambao hautaweza kuangushwa, wala kushindwa na
watu wengine. Utazivunja falme zingine vipande vipande na kuzikomesha zote,
nao utadumu milele. 45 Kama tu ulivyoona, jiwe lilichongwa kutoka katika mlima,
lakini si kwa mikono ya wanadamu. Lilivunja vunja chuma, shaba, udongo,
fedha, na dhahabu katika vipande vipande. Mungu mkuu amekujulisha wewe,
mfalme, kile kitakachotokea baada ya haya. Ndoto ni ya kweli na tafsiri yake ni
ya kuaminika. 46 Mfalme Nebukadneza alianguka kifudifudi mbele ya Daniel na
alimweshimu; aliamuru kwamba sadaka zitolewe na manukato yatolewe kwake.

47 Mfalme alimwambia Danieli, " Hakika Mungu wako ni Mungu wa miungu, Bwana
wa wafalme, na ambaye hufunua mafumbo, kwa kuwa umekuwa ukiweza kufumbua
mafumbo haya." 48 Ndipo mfalme alimfanya Danieli kuwa wa kuheshiwa sana na
alimpa zawadi nyingi nzuri. Alimfanya kuwa mtawala juu ya jimbo lote la Babeli.
Danieli akawa liwali mkuu juu watu wenye hekima wa Babeli. 49 Danieli alipeleka
ombi kwa mfalme, na mfalme aliwateua Shadraka, Meshaki na Abedinego kuwa
watawala juu ya jimbo la Babeli. Lakini Danieli alisalia katika ikulu ya mfalme.

# 3

1 Mfalme Nebukadneza alitengeneza sanamu ya dhahabu ambayo ilikuwa na urefu
wa dhiraa sitini na upana dhiraa sita. Aliiweka katika uwanda wa Dura katika
jimbo la Babeli. 2 Kisha Nebukadneza alituma ujumbe wa kuwaita pamoja magavana
wote wa majimbo, magavana wa mikoa, na magavana wa vijiji, pamoja na na
washauiri, wahazini, waamuzi, mahakimu, na maafisa wengine wakuu wa majimbo
ili waje kwa ajili ya uzinduzi wa sanamu aliyokuwa ameiweka. 3 Ndipo magavana
wa majimbo, magavana wa mikoa, na magavana wa vijiji, pamoja na washauri,
wahasibu, waamuzi, mahakimu, na maafisa wa juu wa majimbo walikusanyika kwa
pamoja katika uzinduzi wa sanamu ambayo Nebukadneza aliyokuwa ameiweka.
Walisimama mbele yake. 4 Kisha mtangazaji alipiga kelele, "Enyi watu, mataifa,
na lugha mmeamriwa 5 kwamba mtakaposikia sauti za pembe, filimbi, ala za
muziki, zeze, vinubi na zumari na aina zote za muziki, ni sharti kuanguka na
kuisujudia ninyi wenyewe sanamu ya dhahabu ambayo Mfalme Nebukadneza
alikuwa ameiweka. 6 Na yeyote asiyeanguka na kuiabuda, kwa wakati huo huo
atatupwa katika tanuru la moto." 7 Basi watu walilposikia sauti za pembe, filimbi,
ala za muziki, zeze, vinubi na zumari na aina zote za muziki, watu wote, mataifa
na lugha walianguka na kuisujudia wao wenyewe sanamu ya dhahabu ambayo
Nebukadneza mfalme alikuwa ameiweka. 8 Wakati huu baadhi ya Walkadayo
walikuja na kuleta mashitaka kinyume na Wayahudi. 9 Walimwambia mfalme
Nebukadneza, "mfalme aishi milele! 10 Ewe mfalme, umeweka amri kwamba kila
mtu aisikiye sauti ya pembe, filimbi, ala za muziki, zeze, vinubi na zumari, na aina
zote za muziki, lazima kuanguka na kuisujudia sanamu ya dhahabu. 11 Mtu yeyote
asiyeanguka na kuiabudu sharti atupwe katika tanuru linalowaka moto. 12 Sasa
kuna baadhi ya Wayahudi ambao umewaweka juu masuala ya jimbo la Babeli;
majina yao ni Shadraka, Meshaki, na Abednego. Mfalme, hawa watu hawakutii
wewe. Hawataiabudu, kuitumikia wala kuisujudia wenyewe sanamu ya dhahabu
ambayo umeiweka." 13 Ndipo Nebukadneza alijawa na hasira na ghadhabu, aliagiza
kwamba Shadraka, Meshaki na Abednego waletwe kwake. Hivyo, waliwalete hawa
watu mbele ya mfalme. 14 Nebukadneza aliwaambia, "Je mmejipanga katika akili
zenu, enyi Shadraka, Meshaki na Abedinego, kwamba hamtaiabudu miungu yangu
wala kuisujudia wenyewe sanamu ile ya dhahabu ambayo nimeiweka? 15 Basi sasa
kama mko tayari - mtakaposikia sauti pembe, filimbi, ala za muziki, zeze, vinumbi
na zumari, aina zote za muziki - kuanguka chini na kuisujudia wenyewe sanamu ile
ambayo nimeitengeneza, mambo yote yatakuwa mazuri. Lakini kama hamtaiabudu,
mtatupwa mara katika tanuru la moto. Ni mungu gani atakayeweza kuwaokoa
katika mikono yangu?" 16 Shadraka, Meshaki, na Abednego wakamjibu mfalme,
"Nebukadneza, hatuhitaji kukujibu wewe katika jambo hili. 17 Kama kuna jibu, ni
kwamba Mungu wetu ambaye tunamtumikia anaweza kutuhifadhi sisi salama katika
katika tanuru la moto, na atatuokoa sisi katika mkono wako, mfalme. 18 Kama sivyo,
na ijulikane kwako, wewe mfalme, kwamba hatutaiabudu miungu yako, na wala
hatutaisujudia wenyewe sanamu ya dhahabu uliyoiweka. 19 Ndipo Nebukadneza

alijawa na ghadhabu; mwonekano wa uso wake ulibadilika kinyume na Shadraka, Meshaki na Abedinego. Aliagiza kuwa tanuru lichochewe ukali mara saba zaidi kuliko lilivyokuwa kawaida.
[20] Kisha aliwaamuru baadhi ya watu wenye nguvu katika jeshi lake kuwafunga Shadraka, Meshaki na Abednego na kuwatupa katika tanuru liwakalo moto.
[21] Walifungwa akali wakiwa wamevaa nguo zao, kanzu, kilemba, na mavazi mengine, na walitupa katika tanuru liwakalo moto.
[22] Kwasababu ya agizo la mfalme lilifuatwa na tanuru lilikuwa na joto sana, miali ya moto iliwaua watu waliowatupa Shadraka, Meshaki, na Abedinego.
[23] Hawa wanaume watatu, Shadraka, Meshaki, na Abednego, waliangukia katika tanuru liwakalo moto wakali wamefungwa.
[24] Kisha Nebukadneza mfalme alishangazwa na alisimam haraka. Aliwauliza washauri wake, "Je hatukutupa watu watatu wakiwa wamefungwa katika moto?" Nao walimjibu mfalme, "Hakika mfalme."
[25] Alisema, "Lakini ninaona watu wanne ambao hawajafungwa wakizunguka katika moto, na hawajaumizwa. Mng'ao wa mtu wa nne ni kama mwana wa miungu."
[26] Ndipo Nebukadneza aliposogea karibu na mlango wa tanuru liwakalo moto na akaaita, "Shadraka, Meshaki na Abednego, watumishi wa Mungu Aliye Juu, tokeni nje! Njooni hapa! Ndipo Shadraka, Meshaki na Abednego walitoka nje ya moto.
[27] Magavana wa majimbo, magavana wengine, na washauri wa mfalme waliokuwa wamekusanyika kwa pamoja waliwaona watu hawa. Moto haukuunguza miili yao; nywele katika vichwa vyao hazikuungua; mavazi yao yalikuwa hayajaharibiwa; na hawakuwa na harufu ya moto.
[28] Nebukadneza alisema, "Na tumsifu Mungu wa Shadraka, Meshaki na Abedinego, ambaye amemtuma mjumbe wake na amewapa ujumbe watumishi wake. Walimtumaini yeye wakati walipoikana amri yangu, na waliitoa miili yao badala ya kuabudu au kusujudia mungu mwingine isipokuwa Mungu wao.
[29] Hivyo basi ninaagiza kwamba watu wote, taifa au lugha ambayo itazungumza kitu chochote kinyume na Mungu wa Shadraka, Meshaki na Abedinego lazima wakatwe vipande, na ya kwamba nyumba zao lazima zifanywe kuwa vichuguu vya uchafu kwasababu hakuna mungu mwingine anayeweza kuokoa kama hivi."
[30] Ndipo mfalme aliwapandisha cheo Shadraka, Meshaki na Abednego katika jimbo la Babeli.

# 4

[1] Mfalme Nebukadneza aliituma amri hii kwa watu wote, mataifa, na lugha walioishi katika nchi: "Na amani yenu na iongezeke.
[2] Imeonekana vizuri kwangu kuwaambia juu ya ishara na maajabu ambayo Mungu Mkuu Aliye juu amenifanyia.
[3] Ni kwa namna gani Ishara zake ni kubwa, na ni kwa namna gani maajabu yake yana nguvu! Ufalme wake ni ufalme unaodumu milele, na utawala wake hudumu kizazi hadi kizazi."
[4] Mimi, Nebukadneza, nilikuwa ninaishi kwa furaha katika nyumba yangu, na nilikuwa nikifurahia mafanikio katika ikulu yangu.
[5] Lakini ndoto niliyoiota ilifanya niogope. Nilipokuwa nimejilaza pale, taswira niliyoiona na maono katika akili yangu yalinitaabisha.
[6] Basi nilitoa agizo la kuwaleta mbele yangu watu wote wa Babeli waliokuwa na hekima ili kwamba waweze kunitafsiria ndoto.
[7] Kisha walikuja wachawi, wale ambao hudai kuzungumza na wafu, watu wenye hekima, na wasoma nyota. Niliwaambia juu ya ndoto, lakini hawakuweza kunitafsiria.
[8] Bali mwishoni Danieli aliingia ndani - yeye ambaye huitwa Belteshaza jina la mungu wangu, na ambaye ndani yake kuna roho ya miungu mitakatifu - na nilimwambia juu ya ndoto.
[9] "Belteshaza, mkuu wa wachawi, ninajua kuwa roho ya miungu watakatifu iko ndani yako na ya kwamba hakuna siri iliyo ngumu kwako. Niambie kile nilichokiona katika ndoto yangu na nini maana yake.
[10] Haya ndiyo niliyoyaona katika akili zangu nilipokuwa nimejilaza katika kitanda changu: Nilitazama, na kulikuwa na mti katikati ya dunia, na urefu wake ulikuwa ni mkubwa

sana. 11 Mti ulikua na ukawa wenye nguvu. Na sehemu ya juu yake ilifika mbinguni,
uliweza kuonekana kutoka miisho ya dunia yote. 12 Majani yake yalikuwa mazuri,
matunda yake yalikuwa ni mengi, na juu yake kulikuwa na chakula kwa ajili ya
wote. Wanyama wa mwituni walipata kivuli chini yake, na ndege wa angani waliisha
katika matawi yake. Viumbe vyote hai vililishwa katika mti huo. 13 Nilipokuwa
nimelala kitandani kwangu, niliona katika akili zangu, mjumbe mtakatifu alishuka
kutoka mbinguni. 14 Alipiga kelele na kusema, 'Ukateni mti na yafyekeni matawi yake,
yapukutisheni majani yake, na kuyasambaza matunda yake. Wanyama na wakimbie
kutoka chini yake na ndege wapae mbali kutoka katika matawi yake. 15 Mkiache
kisiki cha mizizi yake katika nchi, mkifunge na fungu la chuma na shaba, katikati
ya mche mororo wa shambani. Na kilowanishwe na umande wa kutoka mbinguni.
Kiacheni kiishi na wanyama kati ya mimea ya ardhini. 16 Akili yake na ibadilishwe
kutoka akili ya kibinadamu, na apewe akili ya mnyama mpaka ipite miaka saba.
17 Uamuzi huu ni kutokana na amri iliyotolewa na mjumbe. Ni uamuzi uliofanya na
yeye aliye mtakatifu ili kwamba hao walio hai wajue kwamba Mungu aliye juu sana
anatawala juu ya falme za watu na huwapa kwa kila mmoja apendaye kumweka
juu yao, hata kwa watu wale wanyenyekevu sana.' 18 Mimi, Mfalme Nebukadneza
nilipata ndoto hii. Sasa, wewe Belteshaza, niambie tafsiri yake, kwasababu hakuna
mtu mwenye hekima katika ufalme wangu anayeweza kunitafsiria. Lakini wewe
unaweza kufanya hivyo, kwa kuwa roho ya miungu watakatifu iko ndani yako."
19 Ndipo Danieli aliyeitwa pia Belteshaza, alihuzunishwa kwa muda, na mawazo
yake yalimshitua. Mfalme akasema, " Belteshaza, usifadhaishwe na ndoto au tafsiri
yake." Belteshaza akajibu, " Bwana wangu, ndoto hii na iwe kwa ajili ya watu
wanaokuchukia, na tafsiri yake na iwe kwa ajili ya adui zako. 20 Mti ule uliouona
- uliokua na ukawa na wenye nguvu, na ambao sehemu yake ya juu ilifika hata
mbinguni, na ambao waweza kuonekana kutoka miisho ya dunia yote - 21 ambao
majani yake ni mazuri, na matunda yake yalikuwa ni mengi, ili kwamba ndani
yake kulikuwa na chakula cha wote, na chini yake wanyama wa mwituni walipata
kivuli, na ndani yake ndege wa angani waliishi - 22 huu mti ni wewe, mfalme, wewe
uliyekua na kuwa na nguvu. Ukuu wako umeongezeka na kufika mbinguni, na
mamlaka yako yamefika hata miisho ya dunia. 23 Ewe mfalme, ulimwona mjumbe
akishuka kutoka mbinguni na akisema, "Ukateni mti na uteketezeni, lakni kiacheni
kisiki cha mizizi yake katika nchi, kifungeni kwa ukanda wa chuma na shaba, katikati
ya mche mororo katika shamba. Na kilowanishwe na umande kutoka mbinguni.
Kiache kiishi katika wanyama wa mwituni katika mashamba mpaka ipite miaka
saba.' 24 Mfalme, hii ni tafsiri yake. Ni agizo la Yeye Aliye Juu ambalo limekufikia,
bwana wangu mfalme. 25 Utafukuzwa utoke miongoni mwa watu, na utaishi pamoja
na wanyama wa mwituni huko mashambani. Utafanywa uwe unakula majani kama
ng'ombe, na utalowanishwa na umande wa kutoka mbinguni, miaka saba itapita
mpaka pale utakapokiri kwamba Mungu Aliye Juu anatawala juu ya falme zote
za watu na ya kwamba yeye humpa falme hizo mtu yeyote amtakaye. 26 Kama
ilivyoamriwa kwamba kukiacha kisiki cha mizizi ya mti, kwa njia hii ufalme wako
utarudishiwa katika kipindi ambacho utajifunza kwamba mbingu inatawala. 27 Hivyo
basi, mfalme, ushauri wangu na ukubalike kwako. Acha kutenda dhambi na utende
haki. Geuka uache uovu wako wa kuonesha huruma kwa walionewa, na itakuwa
kwamba mafanikio yako yataongezwa." 28 Vitu hivi vyote vilitokea kwa mfalme
Nebukadneza. 29 Baada ya miezi wa kumi na miwili alipokuwa akitembea juu ya
dari la ikulu ya kifalme katika Babeli, 30 na alisema, " Je hii si Babeli kuu, ambayo
nimeijenga kwa ajili ya makao yangu ya kifalme, kwa ajili ya utukufu wa enzi yangu?"
31 Wakati maneno yakali katika midomo ya mfalme, sauti ilisikika kutoka mbinguni:

“Mfalme Nebukadneza, imetangazwa kwako kwamba ufalme huu umeondolewa
kutoka kwako. [32] Utafukuziwa mbali kutoka miongoni mwa watu, na makao yao
yatakuwa pamoja na wanyama wa mwitu katika mashamba. Utafanywa kulamajani
kama ng'ombe. Miaka saba itapita mpaka pale utakapokiri kwamba Mungu Aliye Juu
anatawala juu ya falme za watu na humpa falme mtu yeyote amtakaye.” [33] Agizo
hili kinyume na Nebukadneza lilitekelezwa ghafla. Aliondolewa miongoni mwa
watu. Alikula majani kama ng'ombe, na mwili wake ulilowa kwa umande wa kutoka
mbinguni. Nywele zake zilirefuka kama manyoa ya tai, na makucha yake yalikuwa
kama makucha ya ndege. [34] Na katika mwisho wa siku, mimi, Nebukadneza niliinua
macho yangu kuelekea mbinguni, utimamu wa akili nilirudishiwa. “Nilimsifu Mungu
Aliye Juu sana, na nilimheshimu na kumtukuza yeye aishiye milele. Kwa kuwa
utawala wake ni wa milele, na ufalme wake unadumu katoka katika vizazi vyote hadi
vizazi vyote. [35] Wenyeji wote wa duniani huhesabiwa na yeye kuwa bure; hufanya
lolote limpendezalo miongoni mwa jeshi la mbinguni na wakazi wa dunia. Hakuna
hata mmoja awezaye kumzuia au kumpa changamoto. Hakuna hata mmoja awezaye
kumwambia, “Mbona umefanya hivi?” [36] Kwa wakati ule ule utimamu wa akili zangu
uliponirudia, utukufu wangu na fahari yangu ilinirudia kwa ajili ya utukufu wa
ufalme wangu. Washauri wangu na watu wenye heshima walitafuta msaada wangu.
Nilirudishwa kwenye kiti changu cha enzi, na nilipewa ukuu zaidi. [37] Sasa basi, mimi
Nebukadneza, ninamsifu, ninamtukuza na kumheshimu mfalme wa mbinguni, kwa
kuwa matendo yake yote ni ya haki, na njia zake ni za adili. Anaweza kuwashusha
wale wanaotembea katika kiburi chao wenyewe.

# 5

[1] Mfalme Belshaza alifanya sherehe kubwa kwa kwa ajili ya wakuu wake wa
kuheshimiwa wapatao elfu moja, na alikunywa divai mbele yao wote watu elfu
moja. [2] Wakati Belshaza alipokuwa akionja divai, alitoa agizo la kuleta vyombo
vilivyotengenezwa kwa dhahabu au kwa fedha ambavyo Nebukadneza baba yake
alikuwa amevichukua kutoka katika hekalu huko Yerusalemu, ambavyo yeye, na
wakuu wake, na wake zake, na masuria waliweza kuvinywea. [3] Watumishi walivileta
vyombo ya dhahabu vilivyokuwa vimechukulia katika hekalu, nyumba ya Mungu
huko Yerusalemu. Mfalme na wakuu wake, na wake zake na masuria walivinywea.
[4] Walikunywa divai na kuzisifu sanamu zao zilizotengenezwa kwa dhahabu na fedha,
shaba, chuma, mbao na mawe. [5] Kwa wakati huo huo vidole vya mkono wa mtu
vilionekana mbele ya kinara cha taa na kuandika katika ukuta uliopigwa lipu katika
ikulu ya mfalme. Mfalme aliweza kuona sehemu ya mkono ulipokuwa unaandika.
[6] Ndipo uso wa mfalme ulibadilika na mawazo yake yalimwogopesha; miguu yake
haikuweza kumfanya asimame, na magoti yake yalikuwa yakigongana kwa pamoja.
[7] Mfalme alitoa agizo kwa kupiga kelele, waletwe ndani wale ambao hudai wanaweza
kuzungumza na wafu, watu wenye hekima, na wataalamu wa nyota. Mfalme
akawaambia wale waliojulikana kwa hekima katika Babeli, “Yeyote atakayeyaeleza
maandishi haya na maana yake atavikwa nguo za zambarau na atavikwa na mkufu
wa dhahabu shingoni mwake. Naye atakuwa mtawala wa tatu wa juu kwa mamlaka
katika ufalme.” [8] Ndipo watu wote wa mfalme walikuwa wakijulikana kwa hekima
yao waliingia ndani, lakini hawakuweza kuyasoma maandishi wala kueleza maana
yake kwa mfalme. [9] Kisha mfalme Belshaza alishitushwa sana na mwonekano wa uso
wake ulibadilika. Wakuu wake nao walishangazwa sana. [10] Ndipo sasa malkia alikuja
katika nyumba ya sherehe kwasababu ya kile ambacho mfalme na wakuu wake
walikuwa wamekisema. Malkia akasema, “Mfalme na aishi milele! Usiache mawazo
yako yakakusumbua. Usiruhusu mwonekano wa uso wako ubadilike. [11] Kuna mtu

katika ufalme wako ambaye ana roho ya miungu watakatifu dani yake. Katika
siku za baba yako, mwanga na weledi na hekima ya miungu ilipatikana ndani
yake. Mfalme Nebukadneza, baba yako mfalme, alimfanya kuwa mkuu wa waganga,
pamoja na mkuu wa wale wanazungumza na wafu, na wa wenye hekima, na wa
wataalamu wa nyota. 12 Roho bora, ufahamu, weledi, kutafsiri ndoto, kufafanua
mafumbo na kutatua matatizo - hizi ni sifa zilizopatikana kwa mtu huyu Danieli,
ambaye mfalme alimwita Belteshaza. Sasa mwiteni Danieli naye atawaambia maana
ya kile kilichoandikwa." 13 Ndipo Danieli alipoletwa mbele ya mfalme. Mfalme
akamwambia, "Wewe ni yule Danieli, mmoja kati ya watu wa mateka wa Yuda,
ambao baba yangu mfalme aliwaleta kutoka Yuda. 14 Nimesikia habari kukuhusu
wewe, kwamba roho ya miungu iko ndani yako, na ya kwamba mwanga na ufahamu
na hekima bora inapatikana ndani yako. 15 Na sasa watu wanaojulikana kwa hekima
na wale wanaozungumza na wafu, wamekwisha kuletwa mbele yangu, ili kusoma
maandishi haya na kunijulisha maana ya tafsiri yake, lakini hawakuweza kunijulisha
tafsiri yake. 16 Nimesikia kwamba unaweza kutoa tafsiri na kutatua matatizo. Sasa
kama utaweza kusoma maandishi na kuniambia maana yake, utavikwa nguo za
zambarau na kuwa na kuvalishwa mkufu wa dhahabu shingoni mwako, na utakuwa
mtawala wa tatu mwenye mamlaka katika ufalme." 17 Kisha Danieli akajibu mbele
ya mfalme, "Zawadi yako na iwe kwa ajili yako mwenyewe, na thawabu yako na
umpe mtu mwingine. Hata hivyo, mfalme, nitakusomea maandishi na nitakwaambia
maana. 18 Na juu yako, Ewe mfalme, Mungu Aliye juu sana alimpa Nebukadneza baba
yako ufalme, ukuu, heshima na enzi. 19 Na kwasababu ya ukuu huo, Mungu alimpa
watu wote, mataifa, na lugha walimtetemekea na kumwogopa. Aliwauwa wale
aliotaka wafe na aliwaacha hai wale aliotaka waishi. Aliwainua wale aliowataka, na
aliwashusha wale aliowataka. 20 Lakini wakati moyo ulipokuwa na kiburi na roho
yake ilifanywa kuwa mgumu na kwasababu hiyo alitenda kwa kiburi, alishushwa
kutoka kiti chake cha enzi cha kifalme, na waliiondoa enzi yake. 21 Aliondolewa
katika ubinadamu, alikuwa na akili za mnyama, na aliishi na punda wa mwituni.
Alikula majani kama ng'ombe. Mwili wake ulilowanishwa kwa umande wa kutoka
mbinguni mpaka pale alipojifunza kwamba Mungu Aliye Juu anatawala juu ya
falme za watu na ya kwamba humweka mtu yeyote amtakaye juu yake. 22 Wewe
mwana wake, Belshaza, haujaunyenyekeza moyo wako, ingawa aliyajua haya yote.
23 Umejiinua mwenyewe kinyume cha Bwana wa mbinguni. Katika nyumba yake
walikuletea vyombo ambavyo wewe, wakuu wako, wake zako na masuria wako
walivinywea, na kisha ukaisifia sana sanamu zilitengenezwa kwa fedha na dhahabu,
shaba, chuma, mbao, na mawe - sanamu ambazo haziwezi kuona, kusikia wa kujua
kitu chochote. Haujamheshimu Mungu ambaye anaishikilia pumzi yako katika
mkono wake na ambaye anazijua njia zako zote. 24 Ndipo Mungu aliutuma mkono
kutoka katika makao yake na maandishi haya yaliandikwa. 25 Haya ndiyo maandishi
ambayo yaliandikwa: 'Mene, Mene, Tekeli na Peresin.' 26 Maana yake ni: 'Mene,'
'Mungu ameuhesabu ufalme wako na ameukomesha.' 27 'Tekeli' 'umepimwa katika
mizani na umeonekana umepungua.' 28 'Peresi' 'ufalme wako umegawanyika na
wamepewa Wamedi na Waajemi.'" 29 Ndipo Belshaza alitoa agizo, na walimvalisha
Danieli mavazi ya zambarau. Mkufu wa dhahabu walimvisha shingoni, na mfalme
alitoa tamko juu ya Danieli kuwa atakuwa mtawala mwenye mamlaka ya nafasi ya
tatu katika ufalme. 30 Usiku ule Belshaza, mfalme wa Babeli aliuawa, 31 na Dario
Mwajemi aliuchukua ufalme alipokuwa na miaka ipatayo sitini na miwili.

# 6

1 Ilimpendeza Dario kuchagua juu ya ufalme magavana wa majimbo 120 ambao

wangetawala juu ya ufalme wote. 2 Juu yao kulikuwa na watawala wakuu watatu,
na Daniel alikuwa mmoja wao. Hawa watawala waliwekwa ili waweze kuwasimamia
magavana wa majimbo, ili kwamba mfalme asipate hasara. 3 Danieli alipambanuliwa
juu ya watawala wakuu na juu ya magavana wa majimbo kwasababu alikuwa na
roho isiyo ya kawaida. Mfalme alikuwa akipanga kumweka juu ya ufalme wote.
4 Basi watawala wakuu wengine na magavana wa majimbo walitafuta makosa katika
kazi ambazo Danieli alizifanya kwa ufalme, lakini hawakuweza kuona ufisadi au
kushindwa katika majukumu yake kwasababu alikuwa mwaminifu. Hakuna kosa
au uzembe uliopatikana ndani yake. 5 Kisha watu hawa wakasema, "Hatukuweza
kupata sababu yoyote ya kumshitaki huyu Danieli isipokuwa tukitafuta kitu fulani
dhidi yake kuhusiana na sheria za Mungu wake.'" 6 Ndipo watawala hawa na
magavana walileta mpango mbele ya mfalme. Walimwambia, "Mfalme Dario, uishi
milele! 7 Watawala wote wakuu wa ufalme, magavana wa mikoa, na magavana wa
majimbo, washauri, na magavana wameshauriana kwa pamoja na kuamua kuwa
wewe, mfalme, unapaswa kupitisha amri na kuitekeleza, ili kwamba mtu yeyote
anayefanya dua kwa mungu yeyote au mtu kwa siku thelathini, isipokuwa wewe
mfalme, mtu huyo lazima atupwe katika tundu la simba. 8 Sasa mfalme, litoe agizo
na utie saini nyaraka ili kwamba isije ikabadilika, kama ilivyoelekezwa katika sheria
za Wamedi na Waajemi, hivyo haiweze ikabatilishwa. 9 Basi, mfalme Dario alitia
saini nyaraka kwa kuifanya amri kuwa sheria. 10 Danieli alipojua kuwa nyaraka
imekwisha kusainiwa kuwa sheria, alienda ndani ya nyumba yake (madirisha yake
katika chumba cha juu yalikuwa wazi kuelekea Yerusalemu), na alipiga magoti yake,
kama alivyokuwa akifanya mara tatu kwa siku, na aliomba na kushukuru mbele
ya Mungu wake, kama alivyofanya hapo kabla. 11 Kisha watu hawa walikuwa
wameunda hila kwa pamoja walimwona Danieli akiomba na kutafuta msaada kutoka
kwa Mungu. 12 Ndipo walipomwendea mfalme na kuongea naye kuhusiana na
amri yake: "Je haukuweka amri kwamba mtu yeyote akayefanya maombi kwa
mungu mwingine au kwa binadamu ndani ya siku thelathini zijazo, isipokuwa
kwako wewe, mfalme, lazima mtu huyo atupwe katika tundu la simba? Mfalme
akajibu, "Jambo hili ni la hakika, kama ilivyoelekezwa katika sheria za Wamedi na
Waajemi; ambazo haziwezi zikabatilishwa." 13 Kisha wakamjibu mfalme, " Mtu yule
Daniel, ambaye ni mmoja wa watu wa mateka kutoka Yuda, hakutii wewe, mfalme
wala maagizo yako uliyoyasaini. Yeye humwomba Mungu wake mara tatu kwa
siku." 14 Mfalme aliposikia haya, alisikitishwa sana, alitumia akili jinsi ya kumwokoa
kutoka katika utawala huu. Alisumbuka sana mpaka wakati wa kuzama kwa jua
akijaribu kumwokoa Danieli. 15 Kisha watu hawa waliokuwa wamepanga njama
walikusanyika kwa pamoja na mfalme, na wakamwambia, "Ujue mfalme kwamba
ni sheria ya Wamedi na Waajemi kwamba hakuna amri au sanamu ambayo mfalme
anaipitisha yaweza kubadilishwa." 16 Ndipo mfalme alitoa agizo, na walimleta ndani
Danieli, na kisha wakamtupa katika tundu la simba. Mfalme akamwambia Danieli,
"Mungu wako, ambaye unamtumikia daima, na akuokoe.'' 17 Jiwe lililetwa katika
mlango wa tundu, na mfalme alilitia muhuri wa pete yake mwenyewe na pamoja
na muhuri wa wakuu wake ili kwamba chochote kisiweze kubadilishwa kuhusiana
na Danieli. 18 Basi mfalme alienda kwenye ikulu yake na usiku ule alikuwa na
mfungo. Hakuna starehe yoyote iliyoletwa mbele yake, nao usingizi ulimkimbia.
19 Kisha katika mapambazuko mfalme aliamka na kwa haraka alienda kwenye tundu
la simba. 20 Na alipokaribia kwenye tundu, alimwita Danieli kwa sauti ya huzuni,
akimwambia Danieli, "Danieli, mtumishi wa Mungu aliye hai, je Mungu wako ambaye
anamtumkia daima ameweza kukuokoa kutoka katika simba? 21 Ndipo Danieli
akamwambia mfalme, "Mfalme, uishi milele! 22 Mungu wangu amemtuma mjumbe

na amevifunga vinywa vya simba, na hazijaweza kunidhuru. Kwa kuwa sikuwa
na hatia yoyote mbele yake na pia mbele yako, ewe mfalme, na sijakufanyia jambo
lolote la kukudhuru.” 23 Basi mfalme alikuwa na furaha sana. Alitoa agizo kwamba
wanatakiwa wamtoe Danieli nje ya tundu. Hivyo Danieli aliondolewa kutoka katika
tundu. Hakuna dhara lolote lililoonekana kwake, kwa kuwa alikuwa amemtumainia
Mungu wake. 24 Mfalme alitoa agizo, waletwe wale watu waliomshitaki Danieli na
kisha akawatupa wao katika tundu la simba - wao, na watoto wao, na wake zao.
Kabla hawajafika sakafuni, simba waliwararua na kuvunjavunja mifupa yao vipande
vipande. 25 Kisha mfalme Dario aliandika ujumbe kwa watu wote, mataifa na lugha
ambazo ziliishi katika dunia yote: “Amani na iongezeke kwenu. 26 Ninaagiza kwamba
katika utawala wote wa ufalme wangu watu watetemeka na kumcha mbele ya Mungu
wa Danieli, kwa kuwa ni Mungu aliye hai na huishi milele, na ufalme wake hauwezi
kuharibiwa; utawala wake utakuwepo hadi mwisho. 27 Yeye anatuhifadhi salama
na kutuokoa, na anafanya ishara na maajabu mbinguni na duniani; amemhifadhi
Danieli salama dhidi ya uwezo wa simba.” 28 Na hivyo basi, Danieli alifanikiwa katika
utawala wa Dario na katika utawala wa Koreshi Mwajemi.

# 7

1 Katika mwaka wa kwanza wa Belshaza mfalme wa Babelli, Danieli alikuwa
na ndoto na maono katika akili zake wakati alipokuwa amelala kitandani kwake.
Kisha akayaandika yale aliyoyaona katika ndoto. Aliandika matukio ya muhimu
sana: 2 Danieli alieleza, “Usiku katika ndoto zangu niliona pepo nne za mbinguni
zilikuwa zinaitikisa bahari kuu. 3 Wanyama wakubwa wanne, kila mmoja alikuwa
tofauti na mwenzake, walitoka katika bahari. 4 Mnyama wa kwanza alikuwa kama
simba, lakini alikuwa na mabawa ya tai. Nilipokuwa natazama, mabawa yake
yalikuwa yamepasuka na alikuwa ameinuliwa katika ardhi na alikuwa amesimama
kwa miguu miwili kama mtu. Na alipewa akili za kibinadamu. 5 Na kulikuwa na
mnyama wa pili, alikuwa kama dubu, na alikuwa ameinama, alikuwa na mbavu
tatu katikati ya meno yake katika mdomo wake. Aliambiwa, 'Inuka na umeze watu
wangi.' 6 Baada ya hili, niliangalia tena. Kulikuwa na mnyama mwingine ambaye
alionekana kama chui. Mgongoni mwake alikuwa na mabawa manne kama mabawa
ya ndege, na alikuwa na vichwa vinne. Alipewa mamlaka ya kutawala. 7 Baada
haya, niliona usiku katika ndoto yangu mnyama wa nne, mwenye kuogofya, na
kutisha na mwenye nguvu. Alikuwa na meno makubwa ya chuma; aliteketeza, na
kuvunja vunja katika vipande, na kusaga saga katika miguuni pake kile kilichosalia.
Alikuwa ni wa tofauti na wanyama wengine, na alikuwa na pembe kumi. 8 Na wakati
nilipokuwa natafakari juu ya pembe, nilitazama na niliona pembe nyingine ndogo
ilichipuka katikati ya pembe zingine. Mizizi ya pembe tatu kati ya pembe za mwanzo
iling'olewa. Niliona katika pembe hii macho kama macho ya mtu na mdomo ambao
ulikuwa ukijivuna kwa mambo makubwa. 9 Na nilipotazama, viti vya enzi vilikuwa
vimewekwa, na Mtu wa siku za kale alikaa sehemu yake. Mavazi yake yalikuwa
meupe kama theruji, na nywele zake katika kichwa chake zilikuwa safi kama sufu.
Kiti chake cha enzi kilikuwa na miali ya moto, na magurudumu yake yalikuwa
yanawaka moto. 10 Mto wa moto ulitiririka kutoka mbele yake, na mamilioni ya watu
walimtumikia, na wengine mia moja milioni walikuwa wamesimama mbele yake. Na
mahakama iliitishwa, na vitabu vilifunguliwa. 11 Niliendelea kuangalia kwasababu
ya maneno ya kiburi yaliyosemwa na pembe. Nilitazama wakati mnyama anauliwa,
na mwili wake uliharibiwa, na ulitolewa kwa ajili ya kuchomwa moto. 12 Na kwa
wale wanyama wanne waliosalia, mamlaka yao yalitwaliwa mbali, lakini maisha
yao yaliendelezea kwa kipindi fulani cha muda. 13 Katika maono yangu usiku ule,

nilimwona mtu mmoja anakuja katika mawingu ya mbinguni alikuwa kama mwana
wa mtu; alikuja kwa Mzee wa Siku na aliletwa mbele zake. [14] Naye alipewa mamlaka
ya kiutawala na utukufu na mamlaka ya kifalme ili kwamba watu wote, na mataifa
na lugha ziweze kumtumikia yeye. Mamlaka yake ya kutawala ni mamlaka ya milele
ambayo hayatapita, na ufalme wake ni ule ambao hautaangamizwa. [15] Na kwangu
mimi, Danieli, roho yangu ilihuzunishwa ndani yangu, na maono niliyoyaona katika
akili zangu yalinisumbua. [16] Nilimsogelea mmoja wa hawa walikuwa wamesimama
hapo na nikamwomba anioneshe maana ya mambo haya. [17] Hawa wanyama nne
wakubwa ni wafalme wanne ambao watatoa katika nchi. [18] Lakini watu watakatifu
wa Mungu aliyejuu wataupokea ufalme na wataumiliki milele na milele.' [19] Ndipo
nilipotaka kujua zaidi juu ya mnyama wa nne, ambaye alikuwa tofauti sana na
wengine na alikuwa wa kutisha pamoja na meno yake ya chuma na makucha ya
shaba; alimeza, na alivunja vipande vipande, na alisaga saga kwa miguu yake kile
kilichokuwa kimesalia. [20] Nilitaka kujua juu ya pembe kumi katika kichwa chake, na
kuhusu pembe nyingine iliyochomoza, na ambayo mbele yake pembe zingine tatu
zilianguka chini. Nilitaka kujua kuhusu pembe yenye macho na kuhusu mdomo
uliokuwa unajisifu kwa mambo makubwa na ambayo ilionekana kuwa ni kubwa
kuliko zingine. [21] Na nilipotazama, pembe hii iliinua vita dhidi ya watu watakatifu
na ilikuwa inawawashinda mpaka pale [22] Mzee wa Siku alipokuja, na watu watakatifu
wa Mungu Aliye Juu Sana. Ndipo wakati ulipowadia ambapo watu watakatifu
waliupokea ufalme. [23] Hiki ndicho mtu yule alichokisema, 'Kwa habari ya mnyama
wanne, utakuwa ni ufalme wa nne juu ya dunia ambao utakuwa tofauti na falme
zingine zote. Utaimeza dunia yote, na utaikanyaga yote chini na kuivunja vunja
vipande vipande. [24] Na kuhusu pembe kumi, kutoka katika ufalme huu, wafalme
kumi watainuka, na mwingine atainuka baada yao. Atakuwa wa tofauti na wale
waliomtangulia, na atawashinda wale wafalme watatu. [25] Atazungumza maneno
kinyume cha Yeye Aliye Juu sana na atawatesa watu watakatifu wa Mungu Aliye
Juu. Atajaribu kuzibadili sikukuu na sheria. Mambo haya atapewa mikononi mwake
kwa mwaka mmoja, miaka miwili na nusu mwaka. [26] Lakini kikao cha mahakama
kitaitishwa, na watazichukua nguvu zake za kifalme ili mwisho aweza kuharibiwa
na kuteketezwa. [27] Ufalme na utawala, ukubwa wa falme chini ya mbingu yote,
watapewa watu walio wa watu watakatifu wa Yeye Aliye juu Sana. Ufalme wake ni
ufalme wa milele, na falme zingine zote zitamtumikia na kumtii yeye.' [28] Na huu ndio
mwisho wa mambo. Na kuhusu mimi, Danieli, mawazo yangu yanihuzunisha sana
mimi na mwonekano wa uso wangu ulibadilika. Lakini mambo haya niliyahifadhi
mimi mwenyewe."

# 8

[1] Katika mwaka wa tatu wa utawala wa mfalme Belshaza, mimi Danieli niliona
maono (baada ya maono ya awali yaliyonipata). [2] Nilipokuwa nikiangalia katika
ndoto, niliona kwamba nilikuwa katika mji wa Shushani wenye ngome katika
jimbo la Elamu. Niliona katika ndoto kuwa nilikuwa karibu na mfereji wa Ulai.
[3] Nilitazama juu na nikaona mbele yangu kondoo dume lenye mapembe mawili,
limesimama pembeni mwa mfereji. Pembe moja lilikuwa refu kuliko jingine, lakini
pembe ndefu ilikuwa inakua pole pole kuliko ile fupi na pembe fupi ilirefuka na
kuizidi nyingine. [4] Niliona kondoo mme akiishambulia magharibi, kisha kaskazini,
na baadaye kusini; hakuna mnyama mwingine aliyeweza kusimama mbele yake.
Hakuna yeyote aliyeweza kumwokoa yeyote katika mkono wake. Alifanya chochote
kile alichokitaka, na alikuwa mtu mkubwa sana. [5] Na nilipokuwa natafakari juu
ya haya, niliona beberu akitoka magharibi, na kuvuka katika uso wa dunia yote,

akikimbia kwa kasi kana kwamba hakuonekana kama aligusa ardhini. Mbuzi huyo
alikuwa na pembe kubwa katikati ya macho yake. 6 Alienda mpaka kwa kondoo
aliyekuwa na pembe mbili, nilikuwa nimemwona kondoo dume amesimama katika
ukingo wa mfereji na mbuzi alikimbia kumwelekea kondoo dume kwa hasira kali.
7 Niliiona mbuzi ikija karibu na kondoo. Mbuzi alikuwa na hasira na kondoo,
alimpiga kondoo na alizivunja pembe zake mbili. Kondoo hakuwa na nguvu za
kusimama mbele zake. Mbuzi alimgonga kondoo akaanguka chini na akamkanyaga.
Hapakuwa na yeyote wa kumwokoa kutoka katika nguvu zake. 8 Ndipo mbuzi alikua
akawa mkubwa, lakini alipokuwa na nguvu, pembe kubwa ilivunjwa, na katika
sehemu yake zilichipuka na kukua pembe nne kubwa zilizochomoza kuelekea pepo
nne za mbingu. 9 Kutoka katika pembe moja ilichipuka pembe nyingine, ilikuwa
ndogo hapo awali, lakini baadaye ilikuwa pembe kubwa upande wa kusini, na
mashariki, na katika nchi ya uzuri. 10 Pembe ilikuwa kubwa na matokeo yake iliinua
vita dhidi ya jeshi la mbinguni. Baadhi ya jeshi na nyota kadhaa zilitupwa chini
duniani, na zilikanyagwa. 11 Alizidi kuwa mkubwa, mkubwa kama kamanda wa
jeshi la kimungu. Sadaka za kuteketezwa za kila siku ziliondolewa mbali na yeye, na
sehemu yake takatifu zilitiwa unajisi. 12 Kwasababu ya uasi, pembe ya mbuzi ilipewa
jeshi, na sadaka za kuteketezwa zitasitishwa. Pembe itautupa ukweli chini ardhini,
na itafanikiwa katika kila jambo ilifanyalo. 13 Kisha nilimsikia mtakatifu mmoja
akiongea na mtakatifu mwingine akamjibu, " Mambo haya yatadumu kwa muda gani,
maono haya ya sadaka ya kuteketezwa, dhambi ile iletayo uharibifu, ukabidhiajia wa
sehemu takatifu, na jeshi la mbinguni kukanyagwa? 14 Aliniambia, " Itadumu kwa
jioni na asubuhi zipatazo 2, 300. Baada ya hapo, mahali patakatifu patawekwa sawa."
15 Wakati mimi Danieli, nilipoona maono, nilijaribu kuyaelewa. na hapo mbele yangu
alisimama yule aliyeoneakana kama mtu. 16 Niliisikia sauti ya mtu ikiita katikati ya
kingo za mfereji wa Ulai. Alisema, "Gabrieli, msaidie mtu huyu kuelewa maono."
17 Basi alikuja karibu na mahali niliposimama. Na alipokuja, niliogopa na nilisujudia
hadi chini. Aliniambia,"Fahamu, mwana wa mtu, kwamba maono ni kwa ajili ya
wakati wa mwisho." 18 Alipokuwa anaongea na mimi, nilipata usiingizi mzito nikiwa
nimelala kifudifudi. Kisha alinishika na kunisimamisha. 19 Akaniambia, "Tazama,
nitakuonyesha kile kitachotokea baadaye katika kipindi cha ghadhabu, kwasababu
maono haya yanahusu wakati wa mwisho uliopangwa. 20 Na kuhusu kondoo mme
uliyemwona, yule mwenye pembe mbili - ni wafalme wawili wa Umedi na Uajemi.
21 Mbuzi dume ni mfalme wa Ugiriki. Pembe kubwa katikati ya macho yake ni
mfalme wa kwanza. 22 Na kuhusu pembe iliyovunjika, ambayo katika nafasi yake
pembe zingine nne zilichipuka - hizi ni falme nne zitakazoinuka kutoka katika taifa
lake, lakini hazitakuwa na nguvu kubwa. 23 Katika siku zijazo za falme hizo, wakati
ambapo wahalifu watakuwa wamefikia kikomo chao, mfalme mwenye uso katili,
na yeye mwenye akili sana, atainuka. 24 Nguvu zake zitakuwa kubwa, lakini si
kwa nguvu zake mwenyewe. Atakuwa wa kustaajabisha kwa kile atakachokuwa
anakiharibu; atafanya na kufanikiwa. Atawaangamiza watu wenye nguvu, watu
miongoni wa watakatifu. 25 Ataufanya udanganyifu usitawi chini ya mkono wake
kwasababu ya ujanja wake. Atawaangamiza watu wengi bila kutegemea. Atainuka
pia hata kinyume cha Mfalme wa wafalme, na atavunjwa, lakini si kwa mkono
wowote wa binadamu. 26 Maono kuhusu jioni na asubuhi ulizoambiwa ni ya kweli.
Lakini uyafunge maono haya, kwa kuwa yanahusu siku nyingi za wakati ujao.
27 Ndipo mimi, Danieli nilichoka sana na nikalala nikiwa dhaifu kwa siku kadhaa.
Kisha nikainuka na nikaenda kufanya kazi za mfalme. Lakini nilikuwa nimetishwa
sana na maono, na hapakuwa na mtu yeyote aliyeweza kuyaelewa.

# 9

[1] Dario mwana wa Ahasuero, wa uzao wa Wamedi. Alikuwa na Ahasuero ambaye
alifanywa mfalme juu ya ufalme wa watu wa Babeli. [2] Sasa katika mwaka wa
kwanza wa utawala wa Dario, mimi Danieli, nilikuwa najisomea vitabu vilivyo
na neno la Yahweh, neno ambalo lilikuwa limemjia Yeremia nabii. Niligundua
kwamba kungekuwa na miaka sabini hadi mwisho wa kuachwa kwa Yerusalemu
ungefika. [3] Niliugeuza uso wangu kumwelekea Bwana Mungu, ili kumtafuta
yeye kwa sala na maombi, kwa kufunga, na kuvaa nguo za magunia na kukaa
katika majivu. [4] Nilimwomba Yahweh Mungu wangu, na niliungama dhambi zetu.
Nilisema, "Tafadhali, Bwana, wewe ni Mungu mkuu na mwenye kuheshimiwa,
wewe hutunza maagano na uliye mwaminifu katika kuwapenda wale wanaokupenda
wewe na kuzishika amri zako. [5] Tumetenda dhambi na tumefanya yaliyo mabaya.
Tumeenenda kwa uovu na tumeasi, tumegeuka upande kinyume na amri na maagizo
yako. [6] Hatujawasikiliza watumishi wako manabii walizungumza na wafalme wetu,
viongozi wetu, baba zetu, na kwa watu wote wa nchi kwa jina lako. [7] Kwako Bwana,
kuna uadilifu. Hata hivyo, kwetu kuna aibu katika nyuso zetu, kwa watu wa Yuda
na wale wanaoishi Yerusalem, na kwa Israeli yote. Hii ni pamoja na wale walio
karibu na wale walio mbali katika nchi zote ambazo kwazo uliwatawanya. Hii
ni kwasababu ya udanganyifu mkubwa tulioufanya kinyume chako. [8] Kwetu sisi,
Yahweh, kuna fedheha katika nyuso, na kwa wafalme wetu, na kwa viongozi wetu, na
kwa baba zetu, kwasababu tumekutenda dhambi wewe. [9] Kwa Bwana Mungu wetu
kuna huruma na msamaha, kwa kuwa tumemwasi yeye. [10] Hatujaitii sauti ya Yahweh
Mungu wetu kwa kutembea katika sheria zake alizotupatia kupitia watumishi wake
manabii. [11] Israeli wote wameiasi sheria yako na kugeukia upande, kwa kukataa
kuitii sauti yako. Laana na viapo vilivyoandikwa katika sheria ya Musa, mtumishi
wa Mungu, zimemwagwa juu yetu kwa kuwa tummetenda dhambi. [12] Yahweh
ameyathibitisha maneno ambayo aliyasema kinyume na sisi na kinyume na viongozi
wetu juu yetu, kwa kuleta juu yetu janga kubwa. Kwa kuwa chini ya mbingu
yote haijawahi kufanyika kitu chochote ambacho kinaweza kulinganishwa na kile
kilichofanyika huko Yerusalemu. [13] Kama ilivyoandikwa kwenye sheria ya Musa, baa
hili lote limetupata, ingawa bado hatujaomba rehema kutoka kwa Yahweh Mungu
wetu kwa kugeuka na kuacha maovu yetu na kuufuata ukweli wako. [14] Hivyo basi,
Yahweh ameyaweka tayari maafa na ameyaleta juu yetu, kwa kuwa Yahweh Mungu
wetu ni mwenye haki katika matendo yote anayoyafanya, ingawa bado hatujaitii sauti
yake. [15] Basi sasa, Bwana Mungu wetu, uliwatoa watu wako katika nchi ya Misri
kwa mkono wenye nguvu, na umejifanyia jina maarufu kwa ajli yako mwenyewe,
hata siku hii ya leo. Lakini bado tumekutenda dhambi; tumefanya mambo ya hila.
Kwasababu ya matendo yako yote ya haki, [16] Bwana, iache hasira na ghadhabu
yako iwe mbali na mji wako Yerusalemu, mlima wako mtakatifu. Hii ni kwasababu
ya dhambi zetu, na kwasababu ya uovu wa baba zetu, Yerusalemu na watu wako
wamekuwa kitu cha kudharauliwa na wote wanaotuzunguka. [17] Basi sasa, Mungu
wetu, sikiliza sala za mtumishi wako na maombi yake kwa ajili ya rehema; kwa
ajili yako, Bwana ufanye uso wako ung'ae katika sehemu yako takatifu iliyoachwa
ukiwa. [18] Mungu wangu, fungua masikio yako na usikie; fumbua macho yako na
uone. Tumeharibiwa; utazame mji unaoitwa kwa jina lako. Hatukuombi msaada
wako kwasababu ya haki yetu, ila kwasababu ya rehema zako kuu. [19] Bwana, sikiliza!
Bwana, samehe! Bwana, tuangalie na ufanye jambo! Kwa ajili yako mwenyewe,
usichelewe, Mungu wangu, kwa kuwa mji wako na watu wako wanaitwa kwa jina
lako." [20] Nilipokuwa ninaongea kwa kuomba na kuungama dhambi yangu na dhambi
ya watu wangu Israeli, na kuwasilisha maombi yangu mbele ya Yahweh Mungu

wangu kwa niaba ya mlima mtakatifu wa Mungu. [21] Nilipokuwa ninaomba, mtu
Gabrieli, ambaye nilikuwa nimemwona katika ndoto hapo awali, alipaa kwa kasi
kushuka kuja nilipo, ilikuwa ni wakati wa sadaka ya jioni. [22] Alinipa ufahamu na
aliniambia, “Danieli, nimekuja sasa ili nikupe utambuzi na ufahamu. [23] Ulipoanza
kuomba rehema, amri ilitolewa na nimekuja kukueleza jibu, kwa kuwa unapendwa
sana. Hivyo basi, tafakari neno hili na uufahamu ufunuo. [24] Miaka sabini na
saba zimeamriwa kwa ajili ya watu wako na mji wako mtakatifu kukomesha hatia
na kumaliza dhambi, na kuleta haki ya milele, na kutimiza maono na unabii,
na kupaweka wakfu mahali patakatifu sana. [25] Ujue na kufahamu kuwa tangu
kupitishwa kwa amri ya kurudi na kuijenga upya Yerusalemu mpaka ujio wa mpakwa
mafuta (atakayekuwa kiongozi), kutakuwa na majuma saba na majuma sitini na
mbili. Yerusalemu itajengwa pamoja na mitaa yake na handaki, licha ya kuwepo
kwa nyakati za shida [26] Baada ya miaka ya majuma sitini na mbili, mtiwa mafuta
ataharibiwa na atakuwa hana kitu chochote. Jeshi la kiongozi ajaye litauangamiza
mji na mahali patakatifu. Mwisho wake utatatokea kwa gharika, na kutakuwa na
vita hata mwisho. Uharibifu umekwisha amriwa. [27] Atalithibitisha agano pamoja na
watu wengi kwa miaka saba. Katikati ya miaka saba atakomesha dhabihu na sadaka.
Baada ya chukizo la uharibifu atatokea mtu atakayeleta ukiwa. Mwisho kamili na
uharibifu umeamriwa kutokea kwa yeye aliyesababisha ukiwa.”

# 10

[1] Katika mwaka wa tatu wa Koreshi mfalme wa Uajemi, ujumbe ulifunuliwa kwa
Danieli, aliyeitwa pia Belteshaza. Ujumbe huu ulikuwa ni wa kwelil. Ulihusu vita
kuu. Danieli aliufahamu ujumbe alipopata ufumbuzi kutoka katika maono. [2] Katika
siku hizo, mimi Danieli, nilikuwa katika maombolezo kwa wiki tatu. [3] Sikula chakula
kizuri, sikula nyama, sikunywa divai, na sikujipaka mafuta mwenyewe mpaka
ukamilifu wa wiki tatu nzima. [4] Katika siku ya ishirini na nne ya mwezi wa kwanza,
nilipokuwa niko karibu na mto mkubwa (ambao ni Tigrisi), [5] Nilitazama juu na
nikamwona mtu aliyevaa kitani, akiwa na mkanda kiunoni mwake uliotengenezwa
kwa dhahabu safi kutoka Ufazi. [6] Mwili wake ulikuwa kama kito, na sura yake ilikuwa
kama radi. Macho yake yalikuwa kama miali ya tochi, na mikono yake na miguu
yake ilikuwa kama shaba iliyosafishwa. Sauti ya maneno yake ilikuwa kama sauti
ya umati mkubwa wa watu. [7] Mimi, Danieli peke yangu niliyaona maono, na watu
niliokuwa na pamoja hawakuyaona maono. Lakini, jambo kuu la kuogofya liliwaijia
juu yao, na walikimbia na kujificha wao wenyewe. [8] Hivyo niliachwa peke yangu na
niliyaona maono haya ajabu. Hakuna nguvu iliyobakia ndani yangu; mwonekano
wangu wa kung'aa ulibadilika na kuwa mwonekano wa uharibifu, na hazikubakia
nguvu ndani yangu. [9] Kisha nikasikia maneno yake, na nilipoyasikia, nilianguka
kifudifudi na kupata usingizi mzito. [10] Mkono ulinigusa, na ilinifanya nitetemeke
katika magoti yangu na viganja vya mikono yangu. [11] Malaika aliniambia, “Danieli,
mtu aliyetunzwa sana, yafahamu maneno ninayokwambia wewe. Simama wima,
kwa kuwa nimeshakutuma.” Na alipomaliza kuniambia ujumbe huu, nilisimama
nikiwa natetemeka. [12] Kisha aliniambia, “Usiogope, Danieli. Tangu siku ya kwanza
ulipoiweka akili yako kutaka kufahamu na kujinyenyekeza mwenyewe mbele ya
Mungu, maneno yako yalisikiwa, na nimekuja kwasababu ya maneno yako. [13] Mwana
wa mfalme wa ufalme wa Uajemi alinizuia, na niliwekwa huko na mfalme wa
Uajemi kwa siku ishirini na moja. Lakini Mikaeli, mmoja kati ya wakuu alikuja
kunisaidia. [14] Sasa nimekuja kukusaidia ili ufahamu kile kitakachotokea kwa watu
wako katika siku za mwisho. Kwa kuwa maono ni kwa ajili siku ambazo hazijatokea
bado. [15] Na alipokuwa akali akiniambia maneno haya, niligeuza uso wangu na

kuuelekeza chini na sikuwa na uwezo wa kuzungumza. 16 Yeye aliyekuwa kama
wana wa mtu alinigusa mdomo wangu na nifumbua kinywa changu na nilimwambia
huyo aliyekuwa amesimam mbele yangu: “Bwana wangu, niko katika masumbuko
makali kwasababu ya maono; sina nguvu ndani yangu iliyosalia. 17 Mimi ni mtumishi
wako. Je ninawezaje kuongea na Bwana wangu? Kwa kuwa sasa sina nguvu, na
hakuna pumzi iliyosalia ndani yangu.” 18 Tena yule mwenye mwonekano wa mtu
alinigusa na kunitia nguvu. 19 Alisema, “Usiogope, mtu ulithaminiwa sana. Amani
na iwe kwako! Uwe mwenye nguvu, uwe na nguvu!” Na alipokuwa anaongea na
mimi, nilipata nguvu. Nilimwambia, “Bwana wangu na aseme, kwa kuwa umenitia
nguvu.” 20 Aliniambia, “Je unajua ni kwanini nimekuja kwako? Nitarudi hivi
karibuni kupigana na mkuu wa Uajemi. Na nitakapoenda, mkuu wa Ugiriki atakuja.
21 Lakini nitakwambia kile kilichoandikwa katika Kitabu cha Ukweli. Hakuna yeyote
anayejionesha kuwa na nguvu pamoja nami dhidi yao, isipokuwa Mikaeli mkuu
wenu.”

# 11

1 Katika mwaka wa kwanza wa Dario Mmedi, mimi mwenyewe nilikuja kumweze-
sha na kumlinda Mikaeli. 2 Na sasa nitakufunulia ukweli. Wafalme watatu watainuka
katika Uajemi, na mfalme wa nne atakuwa tajiri sana kuliko wengine wote. Na
wakati atakapopata nguvu kupitia utajiri wake, atamwamsha kila mtu kinyume
na ufalme wa Ugiriki. 3 Mfalme wenye nguvu atainuka ambaye atatawala ufalme
mkubwa, na ataenenda kufuatana na matakwa yake mwenyewe. 4 Na atakapokuwa
ameinuka, ufalme wake utavunjika na utagawanyika katika pepo nne za mbinguni,
lakini hawatakuwa wazao wake mwenyewe, na si kwa nguvu zake kwa wakati
alipokuwa akitawala. Kwa kuwa ufalme wake utang'olewa kwa ajili ya wengine
tofauti na wazawa wake. 5 Mfalme wa Kusini atakuwa na nguvu, lakini mmoja kati ya
maamiri jeshi wake atakuwa mwenye nguvu kuliko yeye na atautawala ufalme wake
kwa nguvu kubwa. 6 Baada ya miaka michache, wakati muda utakapokuwa sawa,
watafanya mwungano. Binti wa mfalme wa Kusini atakuja kwa mfalme wa Kaskazini
kuyathibitisha makubaliano yao. Lakini hataweza kuzitunza nguvu za mkono wake,
wala mfalme hatasimama wala mkono wake. Ataachwa na wale waliomleta, na
baba yake, na yeye aliyemwunga mkono katika nyakati hizo. 7 Lakini tawi kutoka
katika mizizi yake litachipuka katika nafasi yake. Atalishambulia jeshi na kuingia
ngome ya mfalme wa Kaskazini. Atapigana nao, na atawashinda. 8 Ataichukua
miungu yao mpaka Misri pamoa na sanamu zao za chuma na vyombo vyao vya
fedha na vya dhahabu vyenye thamani. Kwa miaka mingi atakaa mbali na mfalme
wa Kaskazini. 9 Kisha mfalme wa Kaskazini atauvamia ufalme wa mfalme wa
Kusini, lakini atajitoa na kwenda katika nchi yake mwenyewe. 10 Wana wake
watajiweka tayari na kuunganisha jeshi kubwa. Litaendelea kukua na litagharikisha
kila kitu, litapita katikati hadi kwenye ngome yake. 11 Ndipo mfalme wa Kusini
atakasirika, na ataenda na kupigana naye, mfalme wa Kaskazini. Mfalme wa
Kaskazini atainua jeshi kubwa, bali jeshi litatiwa katika mkono wake. 12 Jeshi
litachukuliwa, na moyo wa mfalme wa Kusini utainuliwa juu, na atawafanya makumi
maelfu kuanguka, lakini hataweza kuwa mshindi. 13 Kisha mfalme wa Kaskazini
atainua jeshi jingine, kubwa kuliko la kwanza. Baada ya miaka kadhaa, mfalme
wa Kaskazini atakuja na jeshi kubwa likiwa na vifaa vingi. 14 Katika siku hizo
wengi watainuka kinyume na mfalmea wa Kusini. Wana wa vurugu miongoni mwa
watu wake watasimama wao wenyewe ili kuyatimiliza maono, lakini watajikwaa.
15 Mfalme wa Kaskazini atakuja, kuizingira nchi kwa kuweka vilima, na kuuteka
mji wenye ngome. Majeshi ya Kusini hayataweza kusimama, hata wanajeshi wake
bora. Hawatakuwa na nguvu za kusimama. 16 Badala yake, yeye ajaye ataenenda

kwa kufuata tamaa zake kinyume chake; hakuna yeyote atakayesimama katika
njia yake. Atasimama katika nchi ya uzuri, na uharibifu utakuwa mkononi wake.
17 Mfalme wa Kaskazini atauelekeza uso wake ili kuja kwa nguvu za ufalme wake
wote, na kutakuwa na makubaliano atakayoyafanya na mfalme wa Kusini. Atampatia
katika ndoa binti wa wanawake ili kuuharibu ufalme wa Kusini. Lakini mpango
huo hautafanikiwa wala kumsaidia. 18 Baada ya hayo, mfalme atafuatilia nchi za
pwani na ataziteka nchi nyingi. Lakini amiri jeshi atakikomesha kiburi chake na
atakisababisha kiburi chake kiishe. 19 Kisha atafuatilia miji yenye ngome katika
nchi yake mwenyewe, lakini atajikwaa na kuanguka; na hatapatikana tena. 20 Kisha
mtu mwingine atainuka katika nafasi ambaye atamfanya mtoza ushuru apite kwa
ajili ya ufahari wa ufalme. Lakini katika siku zijazo atakatiliwa mbali, lakini si
kwa hasira wala si katika vita. 21 Katika nafasi atainuka mtu wa kudharauliwa
ambaye watu hawatampa heshima ya nguvu ya kifalme; atakuja bila kukusudiwa
na atautwaa ufalme kwa ulaghai. 22 Mbele yake, kila jeshi litafutiliwa mbali kama
gharika. Jeshi na kiongozi wa agano wataangamizwa wote kwa pamoja. 23 Tangu
katika kipindi kile ambacho makubaliano yalifanywa pamoja naye, ataenenda kwa
kwa hila; atakuwa mwenye nguvu akiwa na watu wachache tu. 24 Kwa ghafla ataingia
katika sehemu tajiri sana za jimbo, na atafanya kile ambacho si baba yake wala baba
wa baba yake alishakifanya. Atagawanya mateka, nyara, na mali zake miongoni
mwa wafuasi wake. Atapanga mpango wa kuiangusha ngome, lakini ni kwa muda
tu. 25 Ataamsha nguvu zake na moyo wake kinyume na mfalme wa Kusini kwa jeshi
kubwa. Mfalme wa Kusini atapigana vita akiwa na jeshi kubwa lenye nguvu, lakini
hataweza kusimama kwa kuwa wengine watafanya njama dhidi yake. 26 Hata wale
wanaokula chakula chake kizuri watajaribu kumwangamiza. Jeshi lake litakatiliwa
mbali kama gharika, na wengi wao watauawa. 27 Wafalme wote hawa wawili,
wakiwa na mioyo yao imejawa na uovu kinyume na mwenzake, watakaa katika
meza moja na kudanganyana, lakini haitakuwa na maana yoyote. Kwa kuwa mwisho
utatokea katika kipindi ambacho kimeshapangwa. 28 Kisha mfalme wa Kaskazini
atarudi katika nchi yake akiwa na utajiri mkubwa, na moyo wake ukipinga vikali
agano takatifu. Atatenda na kisha atarudi katika nchi yake mwenyewe. 29 Katika
muda uloamriwa atarudi na kuushambulia ufalme wa Kusini. Lakini katika kipindi
hiki hakitakuwa kama awali. 30 Kwa kuwa meli kutoka Kitimu zitamshambulia, naye
ataogopa na kurudi nyuma. Atakuwa mwenye hasira dhidi ya agano takatifu, na
atawaonyesha mema wale watakaoliacha agano takatifu. 31 Majeshi yake yatainuka
na kukufuru sehemu takatifu katika ngome. Wataziondoa sadaka za kawaida za
kuteketezwa, na watasimamisha chukizo la uharibifu litakalosababisha ukiwa. 32 Na
kwa wale walioenenda kwa ouvu kinyume na agano, atawadanganya na kuwatia
uovu. Bali watu wale wanaomjua Mungu wao watakuwa jasiri na watachukua hatua.
33 Watu wenye hekima miongobi mwa watu watawafanya watu waelewe. Lakini
watajikwaa kwa upanga na kwa miali ya moto; watatiwa mateka na kunyang'anywa
kwa siku. 34 Katika siku za kujikwaa kwao, watasaidiwa kwa msaada kidogo. Watu
wengi watajiunga nao wenyewe katika unafiki. 35 Baadhi ya watu wenye hekima
watajikwaa ili kujisafisha kutokee kwao, na kujiosha, na kujitakasa, mpaka wakati wa
mwisho. Kwa kuwa wakati ulioamriwa haujaja bado. 36 Mfalme atafanya kutokana
na matakwa yake. Atajiinua mwenyewe na kujifanya mkubwa kuliko kila mungu.
Kinyume cha Mungu wa miungu, atasema vitu vibaya, kwa kuwa atafanikiwa mpaka
pale ghadhabu itakapokuwa imekamilika. Kwa ajili kile kilichoamriwa kitakapokuwa
kimefanyika. 37 Hatazijali miungu ya baba zake wala mungu anayependwa na
wanawake. Wala hatamjali mungu mwingine yeyote. Kwa kuwa zaidi ya mtu
yeyote atajifanya mwenyewe kuwa mkuu. 38 Atamheshimu mungu wa ngome badala

ya haya. Ni mungu ambaye baba zake hawakumkubali ambaye atamheshimu
kwa dhahabu na fedha, kwa mawe ya thamani na zawadi zenye kuthaminiwa.
39 Atazishambulia ngome imara sana kwa msaada wa mungu mgeni. Atampa
heshima kubwa yeyote anayemkubali. Atawafanya kuwa watawala juu ya watu
wengi, na ataigawanya nchi kama thawabu. 40 Kwa wakati wa mwisho mfalme wa
Kusini atamshambulia. Mfalme wa Kaskazini atamvamia kwa ukali wa magari na
wapanda farasi, na meli nyingi. Naye ataenda kinyume cha nchi, kuwagharikisha,
na kupita katikati. 41 Naye ataingia katika nchi ya uzuri, makumi elfu ya Waisraeli
wataanguka. Lakini watu hawa watatoroka kutoka katika mkono wake: Waedomu,
Wamoabu, na mabaki ya watu wa Amoni. 42 Naye ataunyosha mkono katika nchi;
nchi ya Misri haitaokolewa. 43 Atakuwa na mamlaka juu ya hazina za dhahabu na
za fedha, na juu ya utajiri wote wa Misri; watu wa Libya na Ethiopia watakuwa
chini katika nyayo za miguu yake. 44 Lakini taarifa kutoka mashariki na kaskazini
zitamwogopesha, naye atatoka akiwa mwenye hasira nyingi kuwa ili kuwaharibu
kabisa na kuwahifadhi kwa ajli ya uharibifu. 45 Naye ataisimamisha hema ya makao
yake ya kifalme kati ya bahari na milima ya uzuri wa utakatifu. Ataufikia mwisho
wake, na hapatakuwa na msaidizi wa kumsadia.

# 12

1 Katika kipindi hicho, Mikaeli, jemedari mkuu ambaye huwalinda watu wako,
atainuka. Kutakuwa na wakati wa mateso ambao haujawahi kutokea tangu
mwanzo wa taifa lolote mpaka kipindi hicho. Katika muda huo watu wako
wataokolewa, yeyote ambaye jina lake litapatikana katika kitabu. 2 Na wengi wa
wale waliolala katika mavumbi ya dunia watainuka. baadhi kwa uzima wa milele
na baadhi kwa ajili ya fedheha na matwezo ya milele. 3 Wale wenye hekima
watang'ara kama mng'ao wa anga la juu, na wale wenye kuwaelekeza wengine
katika haki, watakuwa kama nyota milele na milele. 4 Lakini wewe, Danieli,
yafunge maneno haya; kihifadhi kitabu kikiwa kimetiwa chapa mpaka nyakati za
mwisho. Watu wengi watakimbia huku na kule, na maarifa yataongezeka. 5 Kisha
mimi, Danieli, nilitazama, na kulikuwa na malaika wengine wawili wamesimama.
Mmoja alisimama katika upande huu wa ukingo wa mto, na mwingine alisimama
katika ukingo wa upande mwingine wa mto. 6 Mmoja wao alimwambia mtu
aliyevaa nguo za kitani, yeye aliyekuwa juu ya mkondo wa mto, "Je itachukua
muda gani mpaka mwisho wa matukio haya ya kushangaza?" 7 Nilimsikia mtu
yule aliyevaa nguo za kitani, aliyekuwa juu katika mkondo wa mto, aliinua mkono
wake wa kuume na mkono wake wa kushoto kuelekea mbinguni na kuapa kwa
yeye aishiye milele kwamba itakuwa kwa wakati, nyakati, na nusu wakati. Na
wakati nguvu za watu watakatifu zitakapokuwa zimeshaharibiwa, mambo haya
yote yatakuwa yamemalizika. 8 Nilisikia, lakini sikufahamu. Basi nikamwuliza,
"Bwana wangu, mambo haya yote yatakuwa na matokeo gani?" 9 Alisema, "Nenda
zako Danieli, kwa kuwa maneno yamefungwa na kutiwa chapa mpaka wakati wa
mwisho. 10 Watu wengi watakuwa wametakaswa, wameoshwa, na kusafishwa, lakini
waovu wataenenda katika uovu. 11 Katika muda ule ambapo sadaka ya kawaida ya
kuteketezwa itakapokuwa imeondolewa na chukizo la uharibifu liliosababisha ukiwa
limesimamishwa, kutakuwa na siku zipatazo 1, 290. 12 Ana heri mtu yule anayengojea
mpaka mwisho wa siku 1, 335. 13 Unapaswa uondoke uende njia yako hata mwisho,
na kisha utapumzika. Utainuka katika sehemu uliyopewa, mwishoni mwa siku."

# Hosea

1 Hili ni neno la Bwana lililofika kwa Hosea mwana wa Beeri siku za Uzia, Yothamu,
Ahazi na Hezekia, wafalme wa Yuda, na katika siku za Yeroboamu mwana wa
Yoashi, mfalme wa Israeli. 2 Wakati Bwana alipozungumza kwanza kupitia Hosea,
akamwambia, “Nenda ukajitwalie mke ambaye ni kahaba. Atakuwa na watoto
ambao ni matokeo ya ukahaba wake. Kwa maana nchi inafanya uzinzi mkubwa
kwa kumwacha Bwana.” 3 Basi Hosea akaenda akamwoa Gomeri binti Diblaimu,
naye akachukua mimba, akazaa mtoti mwanamume. 4 Bwana akamwambia Hosea,
Mwite jina lake Yezreeli. Kwa maana kwa muda mfupi nitaiadhibu nyumba ya Yehu
kwa sababu ya kumwaga damu huko Yezreeli; nami nitamaliza ufalme wa nyumba
ya Israeli. 5 Itatokea siku ile nitakapovunja upinde wa Israeli katika bonde la Yezreeli.
6 Gomeri akachukua mimba tena akamzaa binti. Ndipo Bwana akamwambia Hosea,
“Mwite jina lake Lo Ruhama; kwa maana sitawahurumia tena nyumba ya Israeli,
nisije nikawasamehe kwa njia yoyote. 7 Hata hivyo nitawahurumia nyumba ya Yuda,
nami nitawaokoa mwenyewe, Bwana, Mungu wao. Sitawaokoa kwa upinde, upanga,
vita, farasi, au wapanda farasi. ' 8 Baada ya Gomeri kumwachisha Lo Ruhama, alipata
mimba na kuzaa mtoto mwingine mwanamume. 9 Ndipo Bwana akasema, “Mwite
jina la Lo Ami; kwa kuwa ninyi si watu wangu, wala mimi si Mungu wenu.” 10 Hata
hivyo idadi ya watu wa Israeli itakuwa kama mchanga wa bahari, ambayo haiwezi
kupimwa au kuhesabiwa. Itakuwa pale ambapo waliambiwa, “Ninyi si watu wangu,”
wataambiwa, “Ninyi ni watu wa Mungu aliye hai.” 11 Watu wa Yuda na watu wa
Israeli watakusanyika pamoja. Wao wataweka kiongozi mmoja wao wenyewe, na
watatoka kutoka nchi, kwa maana itakuwa siku ya Yezreeli kuu.

## 2

1 Waambie ndugu zenu wanaume, 'Watu wangu!' na kwa dada zako, 'umeonyeshwa
huruma.'” 2 Leteni mashtaka dhidi ya mama yenu, leteni mashtaka, kwa kuwa
yeye si mke wangu, wala mimi si mumewe. Na auondoe uzinzi wake mbele yake,
na matendo yake ya uzinzi kati ya matiti yake. 3 Ikiwa sio, nitamvua nguo na
kumuonyesha uchi wake kama siku aliyozaliwa. Nami nitamfanya kama jangwa,
kama nchi iliyoharibika, nami nitamfanya afe kutokana na kiu. 4 Sitakuwa na
rehema kwa watoto wake, kwa maana wao ni watoto wa ukahaba. 5 Maana mama
yao amekuwa kahaba, na yeye aliye mimba amefanya mambo ya aibu. Alisema,
“Nitawafuata wapenzi wangu, kwa maana wananipa mkate wangu na maji, sufu
yangu na kitani, mafuta yangu na kinyweji.” 6 Kwa hiyo nitajenga ua wa kuzuia
njia yake kwa miiba. Nitajenga ukuta dhidi yake ili asiweze kupata njia. Yeye
atawafuatilia wapenzi wake, lakini yeye hatawafikia. 7 Yeye atawatafuta, lakini
hatawapata. Kisha atasema, “Nitarejea kwa mume wangu wa kwanza, kwa maana
ilikuwa ni bora kwangu zamani kuliko sasa.” 8 Kwa maana hakujua kwamba mimi
ndimi niliyempa nafaka, divai mpya na mafuta, na ambaye nilimwongezea fedha
na dhahabu, ambazo walizitumia kwa Baali. 9 Kwa hiyo nitachukua nafaka yake
wakati wa mavuno, na divai yangu mpya katika msimu wake. Nitachukua sufu
yangu na kitambaa kilichotumiwa kufunika uchi wake. 10 Ndipo nitamvua nguo
machoni pa wapenzi wake, wala hakuna mtu atakayemwokoa mkononi mwangu.
11 Nitasitisha furaha yake yote- sikukuu zake, mwandamo wa mwezi, sabato zake na
sikukuu zake zote zilizowekwa. 12 Nitaharibu mizabibu yake na mtini wake, ambayo
alisema, 'Hii ni mishahara ambayo wapenzi wangu walinipa.' Nitawafanya kuwa
msitu, na wanyama wa shambani watakula. 13 Nami nitamuadhibu kwa ajili ya

Sikukuu ya Baali, alipowafukizia uvumba, akijipamba kwa pete zake na mavazi yake,
naye akafuata wapenzi wake, akanisahau." Hili ndilo tamko la Bwana.
14 Kwa hiyo
nitaenda kumshawishi. Nitamleta jangwani na kumwambia kwa huruma.
15 Nami
nitamrudishia mizabibu yake, na bonde la Akori kama mlango wa tumaini. Yeye
atanijibu huko kama alivyofanya katika siku za ujana wake, kama katika siku ambazo
alitoka katika nchi ya Misri.
16 "Itakuwa katika siku hiyo"-hili ndilo tamko la Bwana-
"kwamba utaniita, 'Mume wangu,' na hutaniita tena mimi, 'Baal wangu.'
17 Kwa
maana nitaondoa majina ya Baali kinywani mwake; majina yao hayatakumbukwa
tena."
18 "Siku hiyo nitafanya agano pamoja na wanyama katika mashamba kwa
ajili yao, na ndege wa angani, na vitu vya kutambaa chini. Nitaondoa upinde,
upanga, na vita katika nchi, nami nitakufanya ulale kwa usalama.
19 Nitakuwa
mume wako milele. Nitakuwa mume wako katika haki, hukumu, uaminifu wa
agano, na huruma.
20 Nitakuwa mume wako kwa uaminifu. Nawe utanijua mimi,
Bwana.
21 Na siku ile, nitajibu"-hili ndilo tamko la Bwana. "Nitazijibu mbingu, nao
watajibu dunia.
22 Dunia itashughulikia nafaka, divai mpya na mafuta, na watajibu
Yezreeli.
23 Nitatampanda mwenyewe katika nchi kwa ajili yangu, na nitamhurumia
Lo Ruhama. Nami nitamwambia Lo Ami, 'Wewe ni Ami Ata,' nao wataniambia, 'Wewe
ni Mungu wangu.'"

# 3

1 Bwana akaniambia, "Nenda tena, mpendeni mwanamke, aliyependwa na
mumewe; lakini ni mzinzi. Mpende kama mimi, Bwana, ninavyowapenda watu wa
Israeli, ingawa wanaigeukia miungu mingine na kupenda mikate ya zabibu."
2 Kwa
hiyo nimemnunulia mwenyewe kwa vipande kumi na tano vya fedha na homeri na
letheki ya shayiri.
3 Nilimwambia, "Lazima uishi pamoja nami siku nyingi. Huwezi
kuwa kahaba au kuwa na mtu mwingine yeyote. Kwa njia hiyo hiyo, nitakuwa
pamoja nanyi."
4 Kwa maana wana wa Israeli wataishi kwa siku nyingi bila mfalme,
mtu mkuu, dhabihu, nguzo ya mawe, efodi au sanamu za nyumbani.
5 Baadaye watu
wa Israeli watarudi na kumtafuta Bwana Mungu wao na Daudi mfalme wao. Na
katika siku za mwisho, watakuja wakitetemeka mbele za Bwana na wema wake.

# 4

1 Sikilizeni neno la Bwana, enyi watu wa Israeli. Bwana ana mashtaka dhidi
ya wenyeji wa nchi, kwa sababu hakuna ukweli au uaminifu wa agano, hakuna
ujuzi wa Mungu katika nchi.
2 Kuna laana, uongo, mauaji, wizi na uzinzi. Watu
wamevunja mipaka yote, na damu inakuja baada ya damu.
3 Kwa hiyo nchi
inakauka, na kila mtu aliyeishi ndani yake anaangamia; wanyama katika mashamba
na ndege angani, hata samaki katika bahari, wanaondolewa.
4 Lakini usiruhusu
mtu yeyote kuleta mashtaka; msiruhusu mtu yeyote ahukumu mtu mwingine. Kwa
maana ninyi ndio makuhani, ninaowashtaki.
5 Ninyi makuhani mtajikwaa wakati
wa mchana; manabii pia watajikwaa pamoja nanyi usiku, nami nitamwangamiza
mama yako.
6 Watu wangu wanaharibiwa kwa sababu ya ukosefu wa maarifa.
Kwa sababu makuhani wamekataa maarifa, nami nitawakataa msiwe makuhani
kwangu. Kwa sababu umesahau sheria yangu, ingawa mimi ni Mungu wako, nami
pia nitasahau watoto wako.
7 Makuhani wengi waliongezeka, zaidi walifanya dhambi
dhidi yangu. Walibadilisha heshima zao kwa aibu.
8 Wanajilisha dhambi ya watu
wangu; wao ni wenye tamaa zaidi ya uovu wao.
9 Itakuwa sawa kwa watu kama
kwa makuhani: nitawaadhibu wote kwa matendo yao; Nitawalipa kwa matendo
yao.
10 Watakula lakini hawatashiba; watafanya uzinzi lakini hawataongezeka, kwa
sababu wamekwenda mbali na Bwana.
11 Wanapenda uasherati, divai, na divai

mpya, ambayo imechukua uelewa wao. 12 Watu wangu hutaka shauri kwa sanamu
zao za mbao, na fimbo zao za kutembelea huwapa unabii. Kwa maana mawazo
ya uasherati yamewadanganya, na wamefanya kama makahaba badala ya kuwa
mwaminifu kwa Mungu wao. 13 Wanatoa sadaka juu ya milima na kuteketeza
uvumba kwenye milima, chini ya mialoni, milibua na miela, kwa sababu kivuli ni
nzuri. Basi binti zenu hufanya uasherati, na binti zenu wanazini. 14 Mimi siwaadhibu
binti zako wakati wanachagua kutenda uasherati, wala binti zako wakati wazini. Kwa
maana wanaume pia wanajitoa kwa makahaba, na hutoa dhabihu ili waweze kufanya
vitendo vya uasherati na makahaba. Hivyo watu wasiofahamu wataangamizwa.
15 Ingawa wewe, Israeli, umefanya uzinzi, lakini Yuda asiwe na hatia. Ninyi msiende
Gilgali; msiende hadi Beth Aven. Wala msiape, “Aishivyo Bwana.” 16 Kwa maana
Israeli amefanya ukaidi, kama ndama mkaidi. Je! Bwana anaweza kuwaleta kwenye
malisho kama kondoo mahali penye nafasi? 17 Efraimu alijiunga na sanamu; mwache
peke yake. 18 Hata wakati kileo chao kimeondoka wakaendelea kufanya uzinzi;
watawala wake hupenda sana aibu yao. 19 Upepo utamfunga kwa mabawa yake;
nao wataona aibu kwa sababu ya dhabihu zao.

# 5

1 Sikilizeni haya, makuhani! kuweni makini, nyumba ya Israeli! Sikilizeni, nyumba
ya mfalme! Kwa maana hukumu itakuja juu yenu nyote. Mmekuwa mtego huko
Mizpa na wavu uliosambazwa juu ya Tabori. 2 Waasi husimama sana katika mauaji,
lakini nitawaadhibu wote. 3 Najua Efraimu, na Israeli hajajificha kwangu. Efraimu,
sasa umekuwa kama kahaba; Israeli ni unajisi. 4 Matendo yao hayawataruhusu
kumgeukia Mungu, maana mawazo ya uzinzi yako ndani yao, na hawatamjua Bwana.
5 Kiburi cha Israeli kinawashuhudia; Kwa hiyo Israeli na Efraimu watajikwaa kwa
hatia zao; na Yuda pia wataanguka pamoja nao. 6 Watakwenda pamoja na kondoo
zao na ng'ombe zao kumtafuta Bwana, lakini hawatamuona, kwa kuwa amejiondoa
kutoka kwao. 7 Walikuwa wasio waaminifu kwa Bwana, kwa kuwa wamezaa watoto
haramu. Sasa sherehe mpya za mwezi zitawaangamiza na mashamba yao. 8 Piga
tarumbeta huko Gibea, na tarumbeta huko Rama. Sauti ya kilio cha vita huko Beth
Aveni 'Tutakufuata, Benyamini!' 9 Efraimu itakuwa ukiwa siku ya adhabu. Miongoni
mwa makabila ya Israeli nimetangaza habari itakayotokea. 10 Viongozi wa Yuda ni
kama wale wanaondoao jiwe la mipaka. Nami nitamwaga ghadhabu yangu juu yao
kama maji. 11 Efraimu ameangamizwa; ameangamizwa kwa hukumu, kwa sababu
ametembea kwa hiari kufuata sanamu. 12 Kwa hiyo nitakuwa kama nondo kwa
Efraimu, na kama uozo kwa nyumba ya Yuda. 13 Efraimu alipoona ugonjwa wake,
Yuda akaona jeraha lake; Efraimu akaenda Ashuru; Yuda akatuma wajumbe kwa
mfalme mkuu. Lakini hakuweza kuwaponya watu au kuponya jeraha lako. 14 Kwa
hiyo nitakuwa kama simba kwa Efraimu, na kama simba kwa nyumba ya Yuda. Mimi,
naam mimi, nitapotea na kwenda mbali; Nitawachukua, na hakutakuwa na mtu wa
kuwaokoa. 15 Nitakwenda na kurudi mahali pangu, mpaka watambue hatia yao na
kutafuta uso wangu, hata wakanitafute kwa bidii katika dhiki yao.

# 6

1 “Njoo, turudi kwa Bwana. Kwa maana ametuvunja vipande vipande, lakini
atatuponya; ametujeruhi, lakini atatufunga majeraha yetu. 2 Baada ya siku mbili
atatufufua; siku ya tatu atatuinua, na tutaishi mbele yake. 3 Nasi tumjue Bwana;
tukaendelee kumjua Bwana. Kuja kwake ni hakika kama asubuhi; atakuja kwetu
kama mvua, kama mvua ya vuli ambayo huinyeshea ardhi.” 4 Efuraimu, nikufanyie
nini? Yuda, nikufanyie nini? Uaminifu wako ni kama wingu la asubuhi, kama

umande unaoondoka mapema. 5 Kwa hiyo nimewavunja vipande vipande kwa
vinywa vya manabii, nimewaua kwa maneno ya kinywa changu. Maagizo yako
ni kama nuru inayoangaza. 6 Kwa maana natamani uaminifu wala si dhabihu, na
kumjua Mungu kuliko sadaka za kuteketezwa. 7 Kama Adamu wamevunja agano;
hawakuwa waaminifu kwangu. 8 Gileadi ni jiji la wahalifu wenye miguu ya damu.
9 Kama makundi ya wanyang'anyi wanaomngojea mtu, hivyo makuhani hujiunga
pamoja kufanya mauaji kwa njia ya Shekemu; wamefanya uhalifu wa aibu. 10 Katika
nyumba ya Israeli nimeona jambo baya; Uzinzi wa Efraimu ukopale, na Israeli
ametiwa unajisi. 11 Kwa maana wewe, Yuda, mavuno yameteuliwa, nitakaporudisha
urithi wa watu wangu.

# 7

1 Wakati wowote ninapotaka kuponya Israeli, dhambi ya Efraimu inafunuliwa,
pamoja na matendo maovu ya Samaria, kwa sababu wanafanya udanganyifu;
mwizi huingia, na kundi la wanyang'anyi hushambulia mitaani. 2 Hawatambui
mioyoni mwao kwamba ninakumbuka matendo yao mabaya. Sasa matendo yao
huwazunguka; yapo mbele ya uso wangu. 3 Kwa sababu ya uovu wao wamemfanya
mfalme awe na furaha, na maofisa wao kwa uongo wao. 4 Wote ni wazinzi, kama
tanuru iliyochomwa na mwokaji, ambaye huacha kuuchochea moto tangu kukanda
unga mpaka kuwa chachu. 5 Siku ya mfalme wetu, viongozi walijifanya wagonjwa
na ukali wa divai. Alinyoosha mkono wake kwa wale waliokuwa wakidhihaki.
6 kwa mioyo kama tanuri, wao hupanga mipango yao ya udanganyifu. Hasira zao
hulala usiku wote; asubuhi huwaka juu kama moto. 7 Wote wamepata moto kama
tanuru, na huwaangamiza wale wanaowatawala. Wafalme wao wote wameanguka;
hakuna hata mmoja wao ananiita. 8 Efraimu anajichanganya mwenyewe kati ya
watu. Efraimu ni mkate ambayo haujawahi kugeuzwa. 9 Wageni wamekula nguvu
zake, lakini hajui. Nywele za mvi hunyunyiza juu yake, lakini hajui. 10 Kiburi
cha Israeli kinawashuhudia; hata hivyo, hawajarudi kwa Bwana, Mungu wao, wala
hawakumtafuta licha ya hayo yote. 11 Efraimu ni kama njiwa, baradhuli na asiye
na busara, humwita kwenda Misri, kisha huruka kwenda Ashuru. 12 Wakienda,
nitasambaza wavu wangu juu yao, nami nitawaangusha kama ndege wa angani.
Nitawaadhibu katika kusonga kwao pamoja. 13 Ole wao! Kwa maana wamepotea
kutoka kwangu. Uharibifu unawajia! Wao wameasi dhidi yangu! Napenda
kuwaokoa, lakini waliongea uongo dhidi yangu. 14 Wala hawakunililia kwa moyo
wao wote, lakini wanaomboleza kwenye vitanda vyao. Wanakusanyika kwa ajili ya
nafaka na divai mpya, nao wananiasi mimi. 15 Ingawa niliwafundisha na kuimarisha
mikono yao, sasa wanapanga mabaya dhidi yangu. 16 Wanarudi, lakini harudi
kwangu, Niliye Juu. Wao ni kama upinde usiotumainika. Maofisa wao wataanguka
kwa upanga kwa sababu ya udhalimu wa vinywa. Hii itakuwa ni aibu yao katika
nchi ya Misri.

# 8

1 “Weka tarumbeta katika midomo yako! Tai anakuja juu ya nyumba ya Bwana
kwa sababu watu wamevunja agano langu na waliasi dhidi ya sheria yangu.
2 Wananililia,'Mungu wangu, sisi katika Israeli tunakujua.' 3 Lakini Israeli amekataa
mema, na adui atamfuata. 4 Wameweka wafalme, lakini sio kwa shauri langu.
Wamewafanya wakuu, lakini sikuwa na habari. Kwa fedha zao na dhahabu
wamejifanyia sanamu wenyewe, ili wakatiliwe mbali.” 5 “Ndama yako imekataliwa,
Samaria. Hasira yangu inawaka juu ya watu hawa. Kwa muda gani watakuwa
na hatia? 6 Kwa maana sanamu hii ilitoka Israeli; fundi aliifanya; si Mungu!

Ndama ya Samaria itavunjwa vipande vipande. [7] Kwa maana watu hupanda upepo
na kuvuna kimbunga. Mbegu zilizosimama hazina vichwa; haitoi unga. Ikiwa
itakomaa, wageni watakula. [8] Israeli imemezwa; sasa wanalala kati ya mataifa
kama kitu kisicho na maana. [9] Kwa maana walikwenda Ashuru kama punda wa
mwitu pekee. Efraimu ameajiri wapenzi kwa ajili yake mwenyewe. [10] Hata ingawa
wameajiri wapenzi kati ya mataifa, sasa nitawakusanya pamoja. Wao wataanza
kupotea kwa sababu ya unyanyasaji wa mfalme wa wakuu. [11] Kwa maana Efraimu
imeongeza madhabahu kwa sadaka za dhambi, lakini zimekuwa madhabahu kwa
kufanya dhambi. [12] Niliweza kuandika sheria yangu kwao mara elfu kumi, lakini
wangeiona kama kitu cha ajabu kwao. [13] Kwa ajili ya dhabihu za sadaka zangu,
hutoa nyama na kuila, lakini mimi, Bwana, siwakubali. Sasa nitafikiri juu ya uovu
wao na kuadhibu dhambi zao. Watarudi Misri. [14] Israeli amenisahau mimi, Muumba
wake, na amejenga majumba. Yuda ameimarisha miji mingi, lakini nitatuma moto
juu ya miji yake; itaharibu ngome zake.

# 9

[1] Usifurahi, Israeli, kwa furaha kama watu wengine. Kwa maana haukuwa
mwaminifu, umemuacha Mungu wako. Unapenda kulipa mshahara kwa kahaba
kwenye sakafu zote za nafaka. [2] Lakini sakafu na divai hazitawalisha; divai mpya
itampungukia. [3] Hawawezi kuendelea kuishi katika nchi ya Bwana; badala yake,
Efraimu atarudi Misri, na siku moja watakula chakula kichafu katika Ashuru.
[4] Hawatamtolea Bwana sadaka za divai, wala hawatamfurahisha. Dhabihu zao
zitakuwa kwao kama chakula cha matanga wote wanaolila watakuwa wamejisikia.
Maana chakula chao kitakuwa chao pekee; hautakuingia nyumbani mwa Bwana.
[5] Utafanya nini siku ya sikukuu iliyowekwa rasmi, siku ya sikukuu ya Yahweh? [6] Kwa
maana, angalia, wamekimbia uharibifu, Misri itawakusanya, na Nofu itawazika.
Maana hazina zao za pesa za fedha zitakuwa nao, na miiba itajaza hema zao. [7] Siku
za adhabu zinakuja; siku za kulipiza kisasi zinakuja. Waisraeli wote wajue mambo
haya. Nabii ni mpumbavu, na mtu aliyevuviwa ni mwendawazimu, kwa sababu
ya uovu wako mkubwa na uadui mkubwa. [8] Nabii ndiye mlinzi wa Mungu wangu
juu ya Efraimu. Lakini mtego wa ndege ni juu ya njia zake zote, na uadui umo
katika nyumba ya Mungu wake. [9] Wamejiharibu wenyewe kama siku za Gibea.
Mungu atawakumbusha uovu wao, naye atawaadhibu dhambi zao. [10] Bwana asema,
“Nilipoikuta Israeli, ilikuwa kama kutafuta zabibu jangwani. Kama matunda ya
kwanza ya msimu kwenye mtini, nimewaona baba zenu. Lakini wakaenda Baal
Peori, nao wakajitoa kwenye sanamu ya aibu. Walikuwa chukizo kama sanamu
waliyoipenda. [11] Na kwa ajili ya Efraimu, utukufu wao utatoka kama ndege.
Hakutakuwa na kuzaa, hakuna mimba, wala achukuaye mimba. [12] Ingawa wameleta
watoto, nitawachukua ili asibaki hata mmoja. Ole wao nikiwaacha! [13] Nimeiona
Efraimu, kama vile Tiro, alipandwa katika mlima, lakini Efraimu atatoa watoto
wake kwa mtu atakayewaua. [14] Wape, Bwana-utawapa nini? Wape tumbo lenye
kuharibu mimba na matiti ambayo haitoi maziwa. [15] 'Kwa sababu ya uovu wao
wote huko Gilgali, ndivyo nilipowachukia. Kwa sababu ya matendo yao ya dhambi,
nitawafukuza nje ya nyumba yangu. Sitawapenda tena; maofisa wao wote ni waasi.
[16] Efraimu ni mgonjwa, na mizizi yao imekauka; hawazai matunda. Hata ikiwa wana
watoto, nitawaua watoto wao wapendwa. [17] Mungu wangu atawakataa kwa sababu
hawakumtii. Watakuwa watu wa kutangatanga kati ya mataifa.

# 10

[1] Israeli ni mzabibu mzuri ambao huzaa matunda yake. kwa kadiri matunda

yake yanavyoongezeka vivyo hivyo anajenga madhabahu nyingi. Kwa kuwa nchi
yake ilizalishwa zaidi, aliboresha nguzo zake. 2 Moyo wao ni udanganyifu; sasa
wanapaswa kubeba hatia yao. Bwana ataharibu madhabahu zao; ataharibu nguzo
zao. 3 Kwa maana watasema, “Hatuna mfalme, kwa maana hatukumcha Bwana. Na
mfalme-angeweza kutufanyia nini?” 4 Wanasema maneno tupu na kufanya maagano
kwa kuapa uongo. Kwa hivyo haki inakuja kama magugu yenye sumu katika mito
ya shamba. 5 Wakazi wa Samaria wataogopa kwa sababu ya ndama za Beth Aveni.
Watu wake waliomboleza juu yao, kama walivyofanya wale makuhani wa sanamu
ambao walikuwa wamefurahi juu yao na utukufu wao, lakini hawako tena. 6 Wao
watachukuliwa kwenda Ashuru kama sadaka kwa mfalme mkuu. Efraimu atakuwa
na aibu, na Israeli atakuwa na aibu kwa sanamu yake. 7 Mfalme wa Samaria
ataangamizwa, kama chipu cha kuni juu ya uso wa maji. 8 Sehemu za juu za uovu
zitaharibiwa. Hii ndiyo dhambi ya Israeli! Miti na vichaka vitakua juu ya madhabahu
zao. Watu wataiambia milima, “Tufunike sisi!” na kwa vilima, “Tuangukieni!” 9 Ee
Israeli, umetenda dhambi tangu siku za Gibea; huko umebaki. Je, vita vitawapata
wana wa uovu huko Gibea? 10 Nitakapotaka, nitawaadhibu. Mataifa wataungana
pamoja nao na kuwaweka katika vifungo kwa uovu wao mara mbili. 11 Efraimu
ni ndama mwenye mafunzo ambayo anapenda kupura nafaka, hivyo nitaweka jozi
juu ya shingo yake nzuri. Efraimu nitauweka jozi; Yuda ataimea; Yakobo atauvuta
pigo kwa nafsi yake. 12 Jifanyieni haki, vuneni matunda ya uaminifu wa agano.
Chimbueni ardhi yenu isiyopandwa, kwa maana ni wakati wa kumtafuta Bwana,
mpaka atakapokuja na kuinua haki juu yenu. 13 Mmelima uovu; mmevuna udhalimu.
Mmekula matunda ya udanganyifu kwa sababu uliamini katika mipango yako na
katika askari wako wengi. 14 Kwa hiyo mlipuko wa vita utafufuka kati ya watu wako,
na miji yako yote yenye ngome itaharibiwa. Itakuwa kama Shalmani aliharibu Beth
Arbeli siku ya vita, wakati mama alivunjika vipande vipande na watoto wake. 15 Kwa
hiyo itakuwa kwako, Betheli, kwa sababu ya uovu wako mkubwa. Wakati wa mchana
mfalme wa Israeli atakatwa kabisa.

# 11

1 “Wakati Israeli alikuwa kijana nilimpenda, na nikamwita mtoto wangu kutoka
Misri. 2 Kwa kadiri waliyoitwa, ndivyo walivyoondoka kwangu. Wakawafanyia
dhabihu Baali, wakatafuta uvumba kwa sanamu. 3 Lakini mimi ndio niliyemfundisha
Efraimu kutembea. Ndiye niliyewainua kwa silaha zao, lakini hawakujua kwamba
niliwajali. 4 Niliwaongoza kwa kamba za ubinadamu, na mafungo ya upendo.
Mimi nilikuwa kama mtu aliyepunguza jozi juu ya taya zao, na nikainama na
kuwalisha. 5 Je, hawatarudi nchi ya Misri? Je, Ashuru haitatawala juu yao kwa
sababu wanakataa kurudi kwangu? 6 Upanga utaanguka juu ya miji yao na kuharibu
makomeo ya milango yao; itawaangamiza kwa sababu ya mipango yao wenyewe.
7 Watu wangu wameamua kuniacha. Ingawa wanaita kwa Aliye Juu, hakuna mtu
atawasaidia. 8 Ninawezaje kukuacha, Efraimu? Ninawezaje kukupeleka, Israeli?
Ninawezaje kukufanya kama Adma? Ninawezaje kukufanya kama Seboimu? Moyo
wangu umebadilika ndani yangu; huruma zangu zote zimeongezeka. 9 Sitafanya
hasira yangu kali; Mimi sitawaangamiza Efraimu tena. Kwa maana mimi ni
Mungu, wala si mtu; Mimi ni Mtakatifu kati yenu, nami sitakuja katika ghadhabu.
10 Watanifuata, Bwana. Nitanguruma kama simba. Nami nitaomboleza, na watu
watakuja wakitetemeka kutoka magharibi. 11 Watakuja wakitetemeka kama ndege
kutoka Misri, kama njiwa kutoka nchi ya Ashuru. Nitawafanya wapate kuishi katika
nyumba zao.” Hii ndiyo tamko la Bwana. 12 Efraimu ananizunguka kwa maneno ya

uongo, na nyumba ya Israeli kwa udanganyifu. Lakini Yuda bado anaendelea nami,
Mungu, na ni mwaminifu kwangu, Mtakatifu.

## 12

1 Efraimu hujilisha upepo na kufuata upepo wa mashariki. Yeye daima huzidisha
uongo na unyanyasaji. Wanafanya agano na Ashuru na huchukua mafuta ya Misri.
2 Bwana pia ana mashtaka dhidi ya Yuda na ataadhibu Yakobo kwa yale aliyoyatenda;
atamlipa kwa matendo yake. 3 Katika tumbo Yakobo akamshika ndugu yake kisigino,
na katika ubinadamu wake alijitahidi kwa Mungu. 4 Alishindana na malaika
akashinda. Alilia na kuomba kwa neema yake. Alikutana na Mungu huko Betheli;
huko Mungu aliongea naye. 5 Huyu ndiye Bwana, Mungu wa majeshi; “Yahweh” ndilo
jina lake. 6 Basi tembea kwa Mungu wako. Shika uaminifu na uhuru wa agano, na
umsubiri Mungu wako daima. 7 Wafanyabiashara wana mizani ya uongo mikononi
mwao; wanapenda kudanganya. 8 Efraimu akasema, “Kwa hakika mimi ni tajiri sana;
Nimepata utajiri kwa nafsi yangu. Katika kazi yangu yote hawataona uovu wowote
ndani yangu, chochote ambacho kitakuwa dhambi.” 9 Mimi ndimi Bwana, Mungu
wako, tangu ulipotoka nchi ya Misri. Nitakufanya uishi tena katika hema, kama siku
za karamu iliyowekwa. 10 Niliwaambia manabii, na nimewapa maono mengi kwa
ajili yenu. Kwa mkono wa manabii nilitoa mifano. 11 Ikiwa kuna uovu huko Gileadi,
hakika watu hawafai. Gilgali wanachinja ng'ombe; madhabahu zao zitakuwa kama
miundo ya jiwe katika miamba ya mashamba. 12 Yakobo akakimbia mpaka nchi
ya Aramu; Israeli alifanya kazi ili kupata mke; naye akachunga kundi la kondoo
ili kupata mke. 13 Bwana akawaleta Israeli kutoka Misri kwa kutumia nabii, naye
akawatunza kwa nabii. 14 Efraimu amemkasirisha sana Bwana. Basi Bwana wake
ataachia damu yake, naye atamrudishia aibu yake.

## 13

1 Efraimu alipozungumza, kulikuwa na tetemeko. Alijikuza katika Israeli, lakini
akawa na hatia kwa sababu ya ibada ya Baali, naye akafa. 2 Sasa wanafanya dhambi
zaidi na zaidi. Wanatengeneza sanamu za chuma kutoka kwenye fedha zao, sanamu
kwa kadiri ya ufanisi wao, zote ni kazi ya mafundi. Watu wanasema juu yao, 'Watu
hawa watoao dhabihu na kumbusu ndama.' 3 Kwa hiyo watakuwa kama mawingu ya
asubuhi, kama umande unaoondoka mapema, kama makapi yanayotokana na upepo
kutoka kwenye sakafu, na kama moshi utokao kwenye bomba. 4 Lakini mimi ndimi
Bwana, Mungu weko, tangu nchi ya Misri. Hutamjua Mungu mwingine bali mimi;
wala zaidi yangu, hakuna mkombozi mwingine. 5 Nilikujua jangwani, katika nchi
yenye kame. 6 Wakati ulipokuwa na malisho, ulishiba; na wakati uliposhiba, moyo
wako ukainuliwa. Kwa sababu hiyo umenisahau. 7 Nitakuwa kama simba; kama chui
nitaangalia kando ya njia. 8 Nitawaangamiza kama dubu aliyenyang'anywa watoto
wake. Nami nitararua vifua vyao, na huko nitawaangamiza kama simba, kama vile
mnyama wa mwitu atakayerarua vipande vipande. 9 Nitawaangamiza, Israeli; nani
atakayekusaidia? 10 Mfalme wako yuko wapi, ili akuokoe katika miji yako yote? Wako
wapi wakuu, ambao kwao umeniambia hivi, 'Nipe mfalme na wakuu'? 11 Nimekupa
mfalme kwa hasira yangu, nikamchukua kwa ghadhabu yangu. 12 Uovu wa Efraimu
umehifadhiwa; hatia yake imehifadhiwa. 13 Atakuwa na uchungu wa kujifungua,
lakini ni mwana mjinga, kwa maana wakati wa kuzaliwa, hatatoka tumboni. 14 Je,
nitawaokoa na mkono wa kaburi? Je, nitawaokoa na kifo? Ewe Mauti yako wapi
mapigo yako? Ewe kaburi kuko wapi kuharibu kwako? Huruma itafichwa na macho
yangu. 15 Ingawa Efraimu anafanikiwa kati ya ndugu zake, upepo wa mashariki
utakuja; upepo wa Bwana utapiga kutoka jangwani. Kijito cha maji cha Efraimu

kitauka, na kisima chake hakitakuwa na maji. Adui yake atapora ghala lake la
kila kitu cha thamani. 16 Samaria itakuwa na hatia, kwa sababu amemuasi dhidi
ya Mungu wake. Wataanguka kwa upanga; watoto wao wadogo watavunjwa, na
wanawake wao wajawazito watatambuliwa wazi.

# 14

1 Israeli, rudi kwa Bwana, Mungu wako, kwa kuwa umeanguka kwa sababu ya uovu
wako. 2 Chukueni maneno pamoja nanyi na mrudieni Yahweh. Mwambieni, “Ondoa
uovu wetu wote, uyakubali mema, ili tuweze kukupa matunda ya midomo yetu.
3 Ashuru haitatuokoa; hatutapanda farasi kwenda vitani. Hatuwezi tena kuiambia
kazi ya mikono yetu, 'ninyi ni miungu yetu,' kwa maana kwako mtu asiye na baba
hupata huruma.” 4 'Nitawaponya kugeuka kwao; Nami nitawapenda kwa moyo,
kwa maana hasira yangu itaondoka kwake. 5 Nitakuwa kama umande kwa Israeli;
atachanua kama maua na kuchukua mizizi kama mwerezi nchini Lebanoni. 6 Matawi
yake yataenea; Uzuri wake utakuwa kama mizeituni, na harufu yake kama mierezi
ya Lebanoni. 7 Watu wanaoishi katika kivuli chake watarejea; watafufuliwa kama
nafaka na maua kama mizabibu. Utukufu wake utakuwa kama divai ya Lebanoni.
8 Efraimu, nifanye nini tena na sanamu? Mimi nitamjibu na kumtunza. Mimi ni kama
mberoshi majani yake ni ya kijani daima; kutoka kwangu huja matunda yako.” 9 Nani
mwenye busara ili aelewe mambo haya? Nani anaelewa mambo haya ili awatambue?
Kwa kuwa njia za Bwana ni sawa, na wenye haki watatembea ndani yao, lakini waasi
wataanguka ndani yake.

# Joeli

[1] Hili ni neno la Bwana lililomjia Yoeli mwana wa Pethueli. [2] Sikieni haya, ninyi
wazee, na sikieni, ninyi wenyeji wa nchi. Je! Hii imewahi kuwa kabla ya siku zenu
au katika siku za baba zenu? [3] Waambie watoto wako kuhusu hilo, na waache watoto
wako kuwaambie watoto wao, na watoto wao kizazi kijacho. [4] Yale yaliyosazwa na
tunutu yameliwa na nzige wakubwa; yale yaliyosazwa na nzige panzi wameyala;
na yaliyosazwa na panzi yameliwa na madumadu [5] Amkeni, enyi walevi, lieni!
Omboleza, ninyi nyote mnywao divai, kwa sababu divai nzuri imekatwa kutoka
kwenu. [6] Kwa maana taifa limekuja juu ya nchi yangu, imara na bila idadi. Meno
yake ni meno ya simba, neye ana meno ya simba. [7] Amelifanya shamba langu la
mizabibu kuwa mahali pa kutisha, amechukua mtini wangu. Amechukua gome
lake na kulitupa mbali; matawi yake yamekuwa meupe. [8] Omboleza kama bikira
aliyevaa magunia kwa kifo cha mumewe mdogo. [9] Sadaka ya unga na sadaka ya
kinywaji zimekatiliwa mbali na nyumba ya Bwana. Makuhani, watumishi wa Bwana,
huomboleza. [10] Mashamba yameharibiwa, na nchi imekuwa dhaifu. Kwa maana
nafaka imeharibiwa, divai mpya imekauka, na mafuta yameharibiwa. [11] Oneni aibu,
enyi wakulima, lieni, wakulima wa mzabibu, kwa ngano na shayiri. Kwa mavuno ya
mashamba yameharibika. [12] Mizabibu imeharibika na miti ya mtini imekauka, miti
ya mkomamanga, pia mitende, na miti ya epo - miti yote ya shambani imeharibika.
Kwa furaha imeharibika kutoka kwa wana wa wanadamu. [13] Panda magunia na
omboleza, enyi makuhani! Mwalia, enyi watumishi wa madhabahu. Njoo, ulala usiku
wote kwenye magunia, enyi watumishi wa Mungu wangu. Maana sadaka ya unga
na sadaka ya kinywaji zimezuiliwa nyumbani mwa Mungu wenu. [14] Iteni kwa funga
takatifu, na iteni kusanyiko takatifu. Mkusanyieni wazee na wenyeji wote wa nchi
wafike nyumbani kwa Bwana Mungu wenu, na kumlilia Bwana. [15] Ole kwa siku! Kwa
maana siku ya Bwana imekaribia. Nayo itakuja uharibifu kutoka kwa Mwenyezi.
[16] Je, chakula hakikukatiliwa mbali mbele ya macho yetu, na furaha na kicheko
kutoka nyumbani mwa Mungu wetu? [17] Mbegu zinaoza chini ya udongo wake, ghala
zimekuwa ukiwa, na mabanda yamevunjika, kwa maana nafaka imeharibika. [18] Jinsi
wanyama hulia! Ng'ombe wa ngome wanateseka kwa sababu hawana malisho.
Pia, makundi ya kondoo yanateseka. [19] Bwana, nakulilia wewe. Kwa maana moto
umekula malisho ya jangwani, na moto umeteketeza miti yote ya mashamba. [20] Hata
wanyama wa mashambani wanapanda kwa ajili yako, kwa maana mito ya maji
imekauka, na moto umekula malisho ya jangwani.

## 2

[1] Piga tarumbeta katika Sayuni, na piga kelele juu ya mlima wangu mtakatifu!
Wakazi wote wa nchi watetemeke kwa hofu; maana siku ya Bwana inakuja; Hakika
iko karibu. [2] Ni siku ya giza na weusi, siku ya mawingu na giza nene. Kama asubuhi
inayoenea kwenye milima, jeshi kubwa na la nguvu linakaribia. Hakujawahi kuwako
jeshi kama hilo, na hakutakuwa tena, hata baada ya vizazi vingi. [3] Moto unatumia
kila kitu mbele yake, na nyuma yake moto unawaka. Nchi hiyo ni kama bustani
ya Edeni mbele yake, lakini nyuma yake kuna jangwa lililoharibika. Hakika hakuna
chochote kitakayotoroka. [4] Muonekano wa jeshi ni kama farasi, na wanakimbia kama
wapanda farasi. [5] Wanaruka kwa kelele kama ile ya magari juu ya vilele vya milima,
kama kelele za muale wa moto ambao huangamiza majani, kama jeshi la nguvu
lililo tayari kwa vita. [6] Mbele yao watu wako katika maumivu na nyuso zao zote

zinakuwa za rangi. [7] Wanakimbia kama wapiganaji wenye nguvu; wanapanda kuta
kama askari; wanasonga, kila mmoja kwa hatua, na hawavunji safu zao. [8] Wala
hakuna mmoja anayemsukuma mwingine kando; wanasonga, kila mmoja katika njia
yake; wao huvunja kwa njia ya ulinzi na si kuanguka nje ya mstari. [9] Wanakimbilia
jiji, wanakimbia kwenye ukuta, wanapanda ndani ya nyumba, na hupita kupitia
madirisha kama wezi. [10] Nchi hutikisika mbele yao, mbingu hutetemeka, jua na
mwezi ni giza, na nyota zinaacha kuangaza. [11] Bwana huinua sauti yake mbele ya
jeshi lake; maana wapiganaji wake ni wengi sana; kwa maana wao ni wenye nguvu,
wale wanaofanya amri zake. Kwa maana siku ya Bwana ni kubwa na ya kutisha
sana. Nani anayeweza kuishi? [12] "Lakini hata sasa," asema Bwana, "Nirudieni mimi
kwa mioyo yenu yote. Haraka, lia na omboleza." [13] Rarueni miyoyo yenu, si mavazi
yenu tu, na kurudi kwa Bwana Mungu wenu. Kwa maana ni mwenye neema na
mwenye huruma, si mwepesi wa hasira na wingi katika uaminifu wa agano, na
angependa kugeuka kutokana na adhabu. [14] Nani anajua? Labda angegeuka na
kuwa na huruma, na kuacha baraka nyuma yake, sadaka ya unga na sadaka ya
kinywaji kwa Bwana, Mungu wenu? [15] Piga tarumbeta huko Sayuni, itisha kwa
ajili ya funga takatifu, na itisheni kusanyiko takatifu. [16] Kusanyeni watu, wito
kwa kusanyiko takatifu. Kusanya wazee, kukusanya watoto na watoto wachanga.
Bwana arusi waweze kutoka nje ya vyumba vyao, na bibi arusi kutoka kwenye
vyumba vyao. [17] Basi makuhani, watumishi wa Bwana, waliao kati ya patakatifu
na madhabahu. Wawaambie, Waitie watu wako, Ee Bwana, wala usitoe urithi wako
kwa aibu, ili mataifa watawawale juu yao. Kwa nini wanapaswa kusema kati ya
mataifa, "Yuko wapi Mungu wao?" [18] Ndipo Bwana alikuwa mwenye bidii kwa
nchi yake na kuwahurumia watu wake. [19] Bwana akawajibu watu wake, Tazama,
nitawaletea nafaka, divai mpya, na mafuta. Utaridhishwa nao, wala sitawafanya
kuwa aibu kati ya mataifa. [20] Nitawaondoa washambuliaji wa kaskazini mbali nanyi,
na nitawapitisha katika nchi kavu na iliyoachwa. Sehemu ya mbele ya jeshi lao
itaingia bahari ya mashariki, na sehemuya nyuma itaingia bahari ya magharibi.
Uvundo wake utainuka juu, na harufu yake mbaya itainuka juu. Hakika, amefanya
mambo makuu. [21] Msiogope, nchi, shangilieni na kufurahi, kwa kuwa Bwana
atafanya mambo makuu. [22] Usiogope, wanyama wa kondeni, kwa kuwa malisho
ya jangwa yatakua, miti itazaa matunda yake, na miti ya mizabibu na mizabibu
itazaa mavuno yao yote. [23] Furahini, enyi watu wa Sayuni, na kufurahi katika Bwana,
Mungu wenu. Kwa maana atakupa mvua ya vuli kwa kiasi na kuleta mvua kwa ajili
yenu, mvua ya vuli na mvua ya masika kama hapo awali. [24] Sakafu ya kupepetea
zitajaa ngano, na vyombo vitafurika kwa divai mpya na mafuta. [25] "Nitawawezesha
miaka ya mazao ambayo nzige walikula, Palale, nzige, na nzige wakuteketeza -
jeshi langu lenye nguvu ambalo nimelituma kati yenu. [26] Mutakula chakula tele na
kushiba, na kulitukuza jina la Bwana, Mungu wenu, aliyefanya miujiza kati yenu,
wala sitawaletea tena watu wangu. [27] Utajua ya kwamba mimi niko kati ya Israeli,
na kwamba mimi ni Bwana, Mungu wako, wala hakuna mwingine, wala sitawaletea
aibu watu wangu. [28] Itakuwa baada ya hayo nitamimina Roho yangu juu ya wenye
mwili yote, na wana wenu na binti zenu watatabiri. Wazee wenu wataota ndoto,
vijana wenu wataona maono. [29] Pia juu ya watumishi na watumishi wa kike, siku
hizo nitaimimina Roho wangu. [30] Nitaonyesha maajabu mbinguni na duniani, damu,
moto na nguzo za moshi. [31] Jua litakuwa giza na mwezi kuwa damu, kabla ya siku
kuu na ya kutisha ya Bwana itakapokuja. [32] Itakuwa kwamba kila mtu anayeita jina
la Yahweh ataokolewa. Kwa maana juu ya Mlima Sayuni na Yerusalemu watakuwa
na wale waliokoka, kama Bwana alivyosema, na kati ya wale walisalia, wale ambao
Bwana anawaita.

# 3

1 Tazama, katika siku hizo na wakati huo, nitakaporudi mateka wa Yuda na
Yerusalemu, 2 Nami nitakusanya mataifa yote, na kuwaleta mpaka bonde la
Yehoshafati. Nitawahukumu huko, kwa sababu ya watu wangu na warithi wangu
Israeli, ambao waliwatawanya kati ya mataifa, na kwa sababu waligawanya nchi
yangu. 3 Wamepiga kura kwa ajili ya watu wangu, walinunua kijana kwa ajili
ya kahaba, kuuza msichana kwa divai ili waweze kunywa. 4 Sasa, kwa nini
unanikasirikia, Tiro, Sidoni na mikoa yote ya Wafilisti? Je! mutanirudishia malipo?
Hata kama mutanilipa, mara moja nitawarudishia malipo yenu juu ya vichwa vyenu
wenyewe. 5 Kwa maana mumechukua fedha zangu na dhahabu zangu, nanyi
mukachukua hazina zangu za thamani na kuzileta katika hekalu zenu. 6 Mumewauza
watu wa Yuda na Yerusalemu kwa Wayunani, ili kuwaondoa mbali na maeneo
yao. 7 Tazama, nitawaamsha, watoke mahali ambako muliwauza, na nitawarudishia
malipo juu ya vichwa vyenu wenyewe. 8 Nitawauza wana wako na binti zako, kwa
mkono wa watu wa Yuda. Wao watawauza Sheba, kwa taifa mbali. Kwa maana
Bwana amesema. 9 Tangaza hii kati ya mataifa, 'Jitayarisheni wenyewe kwa ajili ya
vita, waamsheni mashujaa, waacheni wakaribie, mashujaa wote wa vita wapande
juu. 10 Yafueni majembe yenu kuwa panga na visu vyenu vya kuchongea kuwa
mikuki. Basi wadhaifu waseme, 'Nina nguvu.' 11 Haraka na mje, mataifa yote ya
karibu, jikusanyeni pamoja huko. Ee Bwana, washushe mashujaa wako. 12 Naam,
mataifa yajihimize yenyewe kuja hadi bonde la Yehoshafati. Kwa maana nitakaa
huko kuhukumu mataifa yote ya jirani. 13 Wekeni katiki mundu, kwa maana mavuno
yameiva. Njoo, muponde zabibu, kwa ajiri pipa la divai limejaa. Vipuri vilivyofurika,
kwa sababu uovu wao ni mkubwa sana. 14 Kuna mshtuko, mshtuko katika bonde la
Hukumu. Kwa maana siku ya Bwana i karibu katika bonde la hukumu. 15 Jua na
mwezi vinakuwa giza, nyota zimeacha kuangaza. 16 Bwana ataunguruma kutoka
Sayuni, na kuinua sauti yake kutoka Yerusalemu. Mbingu na nchi zitatikisika,
lakini Bwana atakuwa makao kwa ajili ya watu wake, na ngome kwa wana wa
Israeli. 17 Kwa hiyo mtajua ya kuwa mimi ndimi Bwana, Mungu wenu, anayeishi
Sayuni, mlima wangu mtakatifu. Kisha Yerusalemu itakuwa takatifu, na hakuna
jeshi litaklozunguka tena. 18 Katika siku hiyo, milima itatayarisha divai nzuri, milima
itatiririsha maziwa, miito yote ya Yuda itapita katikati ya maji, na chemchemi zitakuja
kutoka nyumba ya Bwana na maji ya bonde la Shitimu. 19 Misri itakuwa ukiwa, na
Edomu itakuwa jangwa tupu, kwa sababu ya vurugu iliyofanyika kwa watu wa Yuda,
kwa sababu walimwaga damu isiyo na hatia katika nchi yao. 20 Lakini Yuda utakua
mwenyeji milele, na Yerusalemu itakuwa kizazi hata kizazi. 21 Nitawalipizia damu
yao, ambayo sijajilipizia kisasi, kwa maana Bwana anaishi Sayuni.

# Amosi

1 Haya ni mambo yanayoihusu Israeli ambayo Amosi, mmoja wa wachungaji katika
Tekoa, aliyapokea katika ufunuo. Alipokea haya mambo katika siku za Uzia mfalme
wa Yuda, na pia katika siku za Yeroboamu mwana wa Yoashi mfalme wa Israeli,
miaka miwili kabla ya tetemeko la aridhi. 2 Alisema, "Yahwe atanguruma kutoka
Sayuni; atainua sauti yake kutoka Yerusalemu. Malisho ya wachungaji yatanyamaza
kimya; kilele cha Karmeli kitanyauka." 3 Hivi ndivyo Yahwe asemavyo: "Kwa dhambi
tatu za Damaskasi, hata kwa nne, sintobadilisha adhabu, kwa sababu wameipura
Gileadi kwa vyombo vya chuma. 4 Nitapeleka moto kwenye nyumba ya Hazaeli, na
utaiteketeza ngome za Ben Hadadi. 5 Nitazivunja komeo za Damaskasi na kumkatilia
mbali mtu ambaye aishiye katika Biqati Aveni, na pia yule mtu ashikaye fimbo ya
kifalme katika Beth Edeni. Na watu wa shamu watakwenda utumwani hata Kiri,"
asema Yahwe. 6 Hivi ndivyo Yahwe asemavyo: "Kwa dhambi tatu za Gaza, hata nne,
sintobadilisha adhabu, kwa sababu waliwachukua mateka watu wote, kuwaweka juu
ya mkono wa Edomu. 7 Nitatuma moto kwenye kuta za Gaza, na kuziteketeza ngome
zake. 8 Nitamkatilia mbali yule mtu aishiye katika Ashdodi na mtu ashikaye fimbo ya
kifalme kutoka Ashkeloni. Nitaugeuza mkono wangu dhidi ya Ekroni, na mabaki ya
Wafilisti wataangamia," asema Bwana Yahwe. 9 Hivi ndivyo Yhawe asemavyo: "Kwa
dhambi tatu za Tiro, hata kwa nne, sintobadili adhabu, kwa sababu waliwapelekea
watu wote wa Edomu, na wamevunja agano lao la undugu. 10 Nitapeleka moto
kwenye kuta za Tiro, nao utaziteketeza ngome zake." 11 Hivi ndivyo Yahwe asemavyo,
"Kwa dhambi tatu za Edomu, hata kwa nne, sintobadilisha adhabu, kwa sababu
alimfuatilia ndugu yake kwa upanga na kutupilia mbali huruma zote. Hasira yake
ikaendelea kuwa kali, na ghadhabu yake ikabaki milele. 12 Nitapeleka moto juu
ya Temani, na utaziteketeza nyumb a za kifalme za Bozra." 13 Hivi ndivyo Yahwe
asemavyo, "Kwa dhambi tatu za watu wa Amoni, hata kwa nne, sintobadilisha
adhabu, kwa sababu wamewapasua wanawake wa Gileadi wenye mimba, ili waweze
kupanua mipaka yao. 14 Nitawasha moto katika kuta za Raba, nao utaziteketeza
nyumba za kifalme, pamoja na kupiga kelele katika siku ya vita, pamoja na dhoruba
katika siku ya kimbunga. 15 Mfalme wao ataenda utumwani, yeye na maafisa wake
pamoja," asema Yahwe.

## 2

1 Hivi ndivyo Yahwe asemavyo: "Kwa dhambi tatu za Moabu, hata kwa nne,
sintobadilisha adhabu, kwa sababu amechoma moto mifupa ya mfalme wa Edomu
hadi kuwa chokaa. 2 Nitatuma moto juu ya Moabu, na utaangamiza ngome za
Keriothi. Moabu atakufa katika gasia, pamoja na kelele na sauti ya tarumbeta.
3 Nitamuharibu mwamuzi kati yake, na nitawaua wana wa mfalme pamoja na
yeye," asema Yahwe. 4 Hivi ndivyo Yahwe asemavyo: "Kwa dhambi tatu za Yuda,
hata kwa nne, sintobadilisha adhabu, kwa sababu wameikataa sheria ya Yahwe na
hawakuzishika amri zake. Uongo wao umesababisha kupotea, ambao baba zao pia
waliufuata. 5 Nitatuma moto juu ya Yuda, na utaimeza ngome ya Yerusalemu." 6 Hivi
ndivyo Yahwe asemavyo: "Kwa dhambi tatu za Israeli, hata kwa nne, sintobadilisha
adhabu, kwa sababu wamewauza wasio na hatia kwa fedha na maskini kwa jozi moja
ya makubadhi. 7 Nao hukanyaga juu ya vichwa vya maskini kama kukanyaga kwenye
mavumbi juu ya aridhi; wanasukuma kukandamiza. Mtu mmoja na baba yake
walilala na msichana mmoja na hivyo kukufuru jina langu takatifu. 8 Nao hulala chini

karibu na kila madhabahu kwenye nguo zilizowekwa dhamana, na katika nyumba ya
Mungu wao hunywa divai ya wale ambao walitozwa faini. 9 Bado nimemwangamiza
Mwamori mbele yao, ambaye urefu wake ulikuwa kama urefu wa mierezi; alikuwa
na nguvu kama mialoni. Kisha nikaharibu matunda yake juu na mizizi yake
chini. 10 Pia, niliwapandisha kutoka nchi ya Misri na kuwaongoza miaka arobaini
nyikani ili mmiliki nchi ya Wamori. 11 Nimewainua manabii kutoka miongoni
mwa watoto wanu wawe Wanadhiri kutoka vijana wenu. Je sio hivyo, watu wa
Israeli? -hivi ndivyo Yahwe asemavyo. 12 Lakini mmewashawishi Wanadhiri kunywa
mvinyo na kuwaamuru manabii wasifanye unabii. 13 Tazama, nitawakanyaga
kama mkokoteni uliojaa miganda inayoweza kumkanyaga mtu. 14 Mtu akimbiaye
hatapata kimbilio; mwenye nguvu hatoongeza nguvu zake mwenyewe; wala shujaa
kujiokoa mwenyewe. 15 Apindaye upinde hatasimama; mkimbiaji sana hatakimbia;
mwendesha farasi hatajiokoa mwenyewe. 16 Hata wapiganaji shujaa watakimbia uchi
katika siku hiyo -hivi ndivyo Yahwe asemavy."

# 3

1 Sikieni neno la Yahwe aliloongea juu yenu, watu wa Israeli, juu ya familia
nzima ambayo niliwatoa kutoka nchi ya Misri, 2 "Nimewachagua ninyi tu kutoka
familia zote za dunia. Kwa hiyo nitawaadhibu kwa dhambi zenu zote." 3 Je wawili
wanaweza kutembea pamoja isipokuwa wamekubaliana? 4 Je simba huunguruma
msituni wakati hakuna mawindo? Je mwana simba ataunguruma kutoka pangoni
mwake kama hajakamata kitu? 5 Je ndege ataanguka kwenye mtego aridhini
wakati hakuna chambo kimewekwa kwa ajili yake? Je mtego utafyatuka juu
aridhini wakati hakuna kitu cha kukamata? 6 Je tarumbeta itapigwa mjini na
watu wasitetemeke? Je janga laweza kuja mjini lisiyoletwa na Yahwe? 7 Hakika
Bwna Yahwe hatafanya kitu vinginevyo amewafunulia mpango watumishi wake
manabii. 8 Simba ameshaunguruma; nani hatoogopa? Bwana Yahwe amekwisha
ongea; nani hatotabiri? 9 Tangaza hii katika ngome huko Ashdodi, na katika ngome
za nchi ya Misri; sema, "Kusanyikeni kwenye milima ya Samaria na oneni vile
mchafuko ulivyomkubwa kwake, na ukandamizaji uliopo katika yeye. 10 Kwa kuwa
hawajui jinsi ya kufanya haki -hivi ndivyo Yahwe asemavyo- hao watunzao nguvu
na uharibifu katika ngome zao." 11 Kwa hiyo, hivi ndivyo Yahwe asemavyo, "Adui
ataizunguka nchi. Atazivuta chini nguvu zako na ngome zenu zitatekwa nyara."
12 Hivi ndivyo Yahwe asemavyo," Kama mchungaji aokoavyo miguu miwili tu kwenye
mdomo wa simba, au kipande cha sikio, ndivyo wana wa Israeli watakavyookolewa
wale waishio katika Samaria, pamoja na pembe ya kulalia, au pembe ya kitanda."
13 Sikieni na kushudia juu ya nyumba ya Yakobo -hivi ndivyo Yahwe asemavyo,
Mungu wa majeshi, 14 "Kwa kuwa katika siku ambayo nimeadhibu dhambi za
Israeli, pia nitaziadhibu madhabahu za Betheli. Pembe za madhabahu zitakatwa
na kuanguka chini. 15 Nitaiharibu nyumba ya baridi pamoja na nyumba ya hari.
Nyumba za pembe zitaangamia, na nyumba kubwa zitatoweka, -hivi ndivyo Yahwe
asemavyo."

# 4

1 Lisikilizeni neno hili, ninyi ng'ombe wa Bashani, ninyi mliomo katika mlima
wa Samaria, ninyi mnaowakandamiza maskini, ninyi mnaowaponda wahitaji, ninyi
muwaambiao waume zenu, "Tuleteeni vinywaji." 2 Bwana Yahwe ameapa kwa
utukufu wake, "Tazama, siku zitakuja kwenu wakati watakapowaondoa kwa ndoana,
wa mwisho wenu na ndoana za kuvulia samaki. 3 Mtatoka kupitia mahali palipo
bomolewa kwenye kuta za mji, kila mmoja wenu kwenda moja kwa moja kupitia

hapo, na mtajitupa mbele ya Harmoni -hivi ndivyo asemavyo Yahwe.” 4 “Nendeni
Betheli na uovu, hata Gilgali mkaongeza dhambi, leteni dhabihu zenu kila asubuhi,
zaka zenu kila baada ya siku tatu. 5 Toeni dhabihu za shukurani pamoja na
mkate; tangazeni sadaka za hiari; watangazieni, kwa kuwa hii ndiyo iwapendezayo,
ninyi watu wa Israeli -hivi ndivyo asemavyo Bwana Yahwe. 6 Nawapatia usafi wa
meno katika miji yenu na na kupungukiwa na mkate katika sehemu zenu zote.
Bado hamkurudi kwangu -hivi ndivyo Yahwe asemavyo. 7 Pia nimeizuia mvua
kutoka kwenu wakati bado kulikuwa na miezi mitatu kwa mavuno. Nikaifanya
inyeshe juu ya mji, na kuifanya isinyeshe katika mji mwingine. Kipande kimoja
cha nchi ilinyesha, lakini kipande kingine cha nchi ambapo haikunyesha palikuwa
pakavu. 8 Walizunguka miji miwili au mitatu kwenda mji mwingine kunywa maji,
lakini hawakutosheka. Bado hawakunirudia mimi -asema Yahwe. 9 Nimewapiga
kwa maradhi yanayosababisha kuvu. Wingi wa bustani, mashamba yenu ya
zabibu, mitini yenu, na mizaituni-kuteketeza yote. Bado hamkunirudia hivi ndivyo
Yahwe asemavyo. 10 Nimetuma tauni kwenu kama ya Misri. Nimewaua watoto
wenu kwa upanga, kubeba farasi zenu, na kuufanya uvundo wa kambi zenu na
kuingiza kwenye pua zenu. Bado hamkunirudia mimi -hivi ndivyo asemavyo Yahwe.
11 Nimeiangamiza miji miongoni mwenu, kama wakati Mungu alipoiangamiza
Sodoma na Gomora. Mlikuwa kama kijinga kilichonyakuliwa kutoka kwenye moto.
Bado hamkunirudia - asema Yahwe. 12 Kwa hiyo nitafanya jambo baya kwako,
Israeli; na kwa sababu nitafanya jambo baya kwako, jiandae kukutana na Mungu,
Israeli! 13 Kwa kuwa, tazama, yeye atangenezaye milima pia ndiye aumbaye
upepo, humfunulia mawazo yake mwanadamu, hufanya asubuhi kuwa giza, na
kupakanyaga mahala pa juu ya dunia. Yahwe, Mungu wa majeshi, ndilo jina lake.”

# 5

1 Sikilizeni hili neno ambalo nisemalo kama maombelezo juu yenu, nyumba ya
Israeli. 2 Bikira wa Israeli ameanguka; hatoinuka tena; ametoroka kwenye nchi yake,
hakuna mtu wa kumwinua. 3 Kwa kuwa hivi ndivyo Yahwe asemavyo: “Mji ambao
umetoka nje kwa elfu watabaki mia, na walioenda nje mia watabaki kumi wa mali ya
nyumba ya Israeli.” 4 Kwa kuwa hivi ndivyo Yahwe asemavyo kwa nyumba ya Israeli:
“Nitafuteni na mtaishi! 5 Msimtafute Betheli; wala kuingia Gilgali; msisafiri kwenda
Bersheba. Kwa kuwa Gilgali watakwenda utumwani hakika, na Betheli haitakuwa
kitu. 6 Mtafuteni Yahwe mtaishi, au atawaka kama moto kwenye nyumba ya Yusufu.
Utateketeza, na hakutakuwa na mtu hata mmoja kuuzima katika Betheli. 7 Wale watu
wageuzao haki kuwa jambo chungu na kuiangusha haki chini!” 8 Mungu aliiumba
Pleidezi na Orioni; amebadilisha giza kuwa asubuhu; hufanya siku kuwa giza na
usiku na kuita maji ya bahari; yeye huyamwaga juu ya uso wa dunia. Yahwe ndilo
jina lake! 9 Yeye huleta uharibifu wa ghafla juu ya waliohodari ili kwamba uharibifu
uje juu ya ngome. 10 Wanamchukia kila awasahihishaye katika lango la mji, nao
humchukia sana yeyote asemaye ukweli. 11 Kwa sababu mnamkanyaga chini maskini
na kuchukua sehemu ya ngano kutoka kwake- ingawa mmejenga nyumba za mawe
yaliyochongwa, hamtaishi kwenye nyumba hizo. Mmependezwa na mashamba ya
mizabibu, lakini hamtakunywa mvinyo wake. 12 Kwa kuwa najua ni jinsi gani mlivyo
na makosa mengi na jinsi dhambi zenu zilivyo kubwa- ninyi mnaowaonea wenye
haki, chukueni rushwa, na kuwageuza wahitaji kwenye lango la mji. 13 Kwa hiyo
kila mtu mwenye busara atanyamaza kimya kwenye wakati kama huo, kwa kuwa ni
wakati wa uovu. 14 Tafuteni mazuri na sio mabaya, ili kwamba mpate kuishi. Hivyo
Yahwe, Mungu wa majeshi, atakuwa na ninyi tayari, kama msemavyo yeye ndiye.
15 Chukieni uovu, imarisheni haki katika lango la mji. Huenda Yahwe, Mungu wa

majeshi, atawafadhili mabaki ya Yusufu. 16 Kwa hiyo, hivi ndivyo Yahwe asemavyo,
Mungu wa majeshi, Bwana, "Kutakuwa na maombolezo kwenye miraba yote, na
watasema kwenye mitaa yote, 'Ole! Ole!' Watawaita wakulima kuomboleza na walio
hodari wa kulia na kuomboleza. 17 Katika mashamba yote ya mizabibu kutakuwa na
kilio, kwa kuwa nitapita katikati yako," asema Yahwe. 18 Ole wenu ninyi mnaoitamani
siku ya Yahwe! Kwa nini mnaitamani? Itakuwa giza na sio nuru, 19 kama wakati
mtu anamkimbia simba na kukutana na dubu, au aliingia katika nyumba na kuweka
mkono wake kwenye ukuta na kung'atwa na nyoka. 20 Je siku ya Yahwe itakuwa
giza na sio nuru? Huzuni na sio furaha? 21 "Nachukia, nazidharau sikukuu zenu,
naichukia mikutano yenu ya dini. 22 Hata kama mnanitolea sadaka ya kuteketeza
na sadaka za unga, sintozipokea, wala kuzitazama kwenye sadaka za ushirika wa
wanyama walionona. 23 Niondoleeni kelele za nyimbo zenu; sintosikiliza sauti za
vinubi vyenu. 24 Badala yake, acheni haki itiririke kama maji, na haki kama mkondo
utiririkao siku zote. 25 Je mmeniletea dhambihu na sadaka za kuteketeza jangwani
kwa mda wa miaka arobaini? 26 Mtamwinua Sikuthi kama mfalme wenu, na Kiuni,
nyota yenu ya miungu-ambayo mmeifanya kwa ajili yenu wenyewe. 27 Kwa hiyo
nitawahamisha upande wa pili wa Damaskasi," asema Yahwe, ambaye jina lake ni
Mungu wa majeshi.

# 6

1 Ole wao wanaostarehe katika Sayuni, na kwa wale ambao wameokoka katika
nchi ya mlima wa Samaria, watu mashuhuri bora wa mataifa, ambao nyumba ya
Israeli huja kwa ajili ya msaada! 2 Viongozi wenu husema, "Pita kwenda Kalne
na mkatazame; kutoka huko nendeni hadi Hamathi, mji mkubwa; kisha nendeni
chini hata Gathi ya Wapelestina. Je ni wabora kuliko falme zenu mbili? Je kuna
mpaka mkubwa kuliko mpaka wenu?" 3 Ole wao wale waiwekao siku ya majanga
na kufanya ufalme kuwa kinyume kusogea karibu. 4 Wamelala juu ya vitanda
vya pembe na kupumzika juu ya viti vyao. Wakala wana kondoo kutoka kwenye
kundi na ndama kutoka kwenye zizi. 5 Wanaimba nyimbo za kijinga kwenye muziki
wa kinubi; wanatunga kwenye vyombo kama vya Daudi. 6 Wanakunywa mvinyo
kutoka kwenye bakuli na kujipaka mafuta wenyewe kwa mafuta ya marahamu, lakini
hawahuzuniki juu ya mateso ya Yusufu. 7 Hivyo sasa watakwenda utumwani pamoja
na watumwa wakwanza, na kelele za hao waliojinyoosha zitapita. 8 "Mimi Bwana
Yahwe, nimeapa kwa nafsi yangu -hivi ndivyo Bwana Yahwe asemavyo, Mungu wa
majeshi, naizira fahari ya Yakobo; nachukia boma zake. Kwa hiyo nitautoa huo mji
pamoja vyote vilivyomo humo." 9 Itakuja kuhusu kwamba kama kuna wanaume
kumi waliobakia kwenye nyumba moja, watakufa. 10 Wakati ndugu wa mtu huyo
atakapokuja kuchukua miili yao-yule ambaye awachomaye baada ya kuleta maiti
katika nyumba-kama akisema kwa mtu katika nyumba, "Je kuna mtu yuko pamoja
nawe?" Vipi kama yule akisema, "Hapana." Kisha atasema, "Kaa kimya, kwa kuwa
hatulitaja jina la Yahwe." 11 Tazama, Yahwe atatoa amri, na nyumba kubwa itapigwa
kuwa vipande vipande, na nyumba ndogo kuwa na nyufa. 12 Je farasi watakimbia
juu ya mteremko wa miamba? Je mtu atalima huko na ng'ome? Bado mmegeuza
haki kuwa sumu na tunda la haki kuwa uchungu. 13 Ninyi mnaofurahia juu ya Lo
Debari, msemao, "Je hatukuchukua Karnaimu kwa nguvu zetu wenyewe?" 14 Lakini
tazama, nitainua juu yenu taifa, nyumba ya Israeli-hivi ndivyo asemavyo Bwana
Yahwe, Mungu wa majeshi. Watawatesa ninyi kutoka Lebo Hamathi hata kijito cha
Araba."

# 7

[1] Hivi ndivyo ambavyo Bwana Yahwe alivyonionyesha. Tazama, aliumba kundi
kubwa la nzige wakati wa kuchipuka kwa mmea, na, tazama, ulikuwa ni mmea wa
mwisho baada ya mavuno ya mfalme. [2] Wakati walipomaliza kula mbogamboga za
nchi, kisha nikasema, “Bwana Yahwe, tafadhali nisamehe; Je Yakobo ataishije? kwa
kuwa yeye ni mdogo sana.” [3] Yahwe akapunguza hasira kuhusu hili. “Haitatokea,”
akasema. [4] Hivi ndivyo ambavyo Bwana Yahwe alivyonionyesha: Tazama, Bwana
Yahwe aliita juu ya moto kuhukumu. Nao ukakausha sana, kilindi chini ya dunia
na kutaka kuitekeza nchi, pia. [5] Lakini nikasema, “Bwana Yahwe, acha tafadhali;
Yakobo ataishije? Kwa kuwa yeye ni mdigo sana.” [6] Yahwe akagairi kuhusiana na hili,
“Hili halitajitokeza pia,” asema Bwana Yahwe. [7] Hivi ndivyo ambavyo Yahwe alivyo
nionyesha: Tazama, Bwana amesimama karibu na ukuta, pamoja na uzi wa timiza
kwenye mkono wake. [8] Yahwe akanambia, “Amosi, unaona nini?” nikasema, “Uzi
wa timazi.” Kisha Bwana akasema, “Tazama, nitaweka uzi wa timazi miongoni mwa
watu wangu Israeli. Sintowaharibu tena. [9] Mahala pa juu pa Isaka pataharibiwa,
patakatifu pa Israeli pataangamia, na nitainuka juu ya nyumba ya Yeroboamu kwa
upanga.” [10] Kisha Amazia, yule kuhani wa Betheli, akatuma ujumbe kwa Yeroboamu,
mfalme wa Israeli: “amosi amefanya njama dhidi yako katikati ya nyumba ya Israeli.
Nchi haiwezi kubeba maneno yote haya. [11] Kwa kuwa hivi ndivyo asemavyo Amosi,
'Yeroboamu atakufa kwa upanga, na hakika Israeli itakwenda utumwani kutoka nchi
yake.”' [12] Amazia akamwambia Amosi, “Mwonaji, nenda, kimbia irudie nchi ya Yuda,
na hapo ule mkate na kutabiri. [13] Lakini usitabiri tena hapa katika Betheli, kwa
kuwa ni patakatifu pa mfalme na nyumba ya kifalme.” [14] Kisha Amosi akamwambia
Amazia, “Mimi sio nabii wala mwana wa nabii. Mimi ni mchungaji wa mifugo,
na mtunza mikuyu. [15] Lakini Yahwe akanichukua kutoka kuchunga mifugo na
kunambia, 'Nenda, katabiri kwa watu wangu Israeli.' [16] Sasa sikia neno la Yahwe.
Wewe usemaye, 'Usitabiri juu ya Israeli, na usiongee juu ya nyumba ya Isaka. [17] Kwa
hiyo hivi ndivyo Yahwe asemavyo, 'Mke wako atakuwa kahaba katika mji; wana wako
waume na binti zako wataanguka kwa upanga; nchi yako itapimwa na kugawanywa;
utakufa katika nchi najisi, na Israeli hakika itakwenda utumwani kutoka nchi yake.”'

# 8

[1] Hiki ndicho ambacho bwana Yahwe amenionyesha. Tazama, kikapu cha matunda
ya hari! [2] Akasema, “Unaona nini, Amosi?” Nikasema, “Kikapu cha matunda ya hari.”
Kisha Yahwe akanambia, “Mwisho umefika kwa watu wangu Israeli; sintowaumiza
tena. [3] Nyimbo za kwenye hekalu zitakuwa vilio. Katika siku hiyo-hivi ndivyo
asemavyo Bwana Yahwe. Mizoga itakuwa mingi, katika kila sehemu wataitupa katika
ukimya!” [4] Lisikilizeni hili, ninyi mkanyagao maskini na kumuondoa fukara wa nchi.
[5] wakisema, “Wakati mwezi mpya utakapoisha, hivyo tunaweza kuuza mazao tena?
Wakati siku ya Sabato itakapoisha, ili kwamba tuuze ngano? Tutafanya kipimo kidogo
na kuongeza bei, tukidanganya kwa mizani za udanganyifu. [6] Hivi ndivyo ambavyo
tunaweza kuuza ngano mbaya, kununua fukara kwa fedha, na masikini kwa jozi
moja ya kubadhi.” [7] Yahwe ameapa kwa fahari ya Yakobo, “Hakika sintoweza
kusahau kazi zao hata moja.” [8] Je nchi haitatetemeka kwa hili, na kila mmoja aishiye
kuombolezea? Yote hayo yatainuka kama Mto Naili, nayo itataabika juu na kupwa
tena, kama mto wa Misri. [9] “Itakuja siku ambayo -huu ndio usemi wa Bwana Yahwe-
kwamba nitafanya jua litue wakati wa mchana, na nitaiweka giza dunia wakati
wa mchana. [10] Nitazigeuza sikukuu zenu kuwa maombolezo na nyimbo zenu zote
kuwa masikitiko. Nitawafanya wote kuvaa nguo za magunia na kipara juu ya kila
kichwa. Nitayafanya haya kama maombolezo kwa mwana pekee, na siku ya uchungu

mwisho wake. [11] Tazama, siku zinakuja -asema Bwana Yahwe- wakati nitakapoleta
njaa katika nchi, sio njaa ya mkate, wala kiu ya maji, ila kusikia maneno ya Yahwe.
[12] watatangatanga kutoka bahari hata bahari; watakimbia kutoka kaskazini kwenda
magharibi kutafuta neno la Yahwe, lakini hawatalipata. [13] Katika siku hiyo wanawali
wazuri na wavulana watazimia kutokana na njaa. [14] Wale waapao kwa dhambi ya
Samaria wataanguka na hawatainuka tena."

# 9

[1] Nilimwona Bwana amesimama karibu na madhabahu, na akasema, "Vipige
vichwa vya nguzo ili kwamba misingi itikisike. Vivunje vipande vipande juu
ya vichwa vyao vyote, nami nitamwua kwa upanga wa mwisho wao. Hakuna
hata mmoja wao atakaye kimbia, hakuna hata mmoja wao atakayekimbia. Hata
kama watachimba kwenye Sheoli, kuna mkono wangu utawachukua. [2] Hata kama
watapanda juu kwenda mbingunu, huko nitawaleta chini. [3] Hata kama watajificha
juu ya Karmeli, nitawatafuta huko na kuwachukua. Hata kama watajificha kwenye
vilindi vya bahari nisiwaone, nimwagiza joka, na atawang'ata. [4] Hata kama wataenda
kwenye utumwa, watabanwa na maadui zao mbele yao, nitauagiza upanga huko, na
utawau. Nitaelekeza macho yangu juu yao kwa ubaya sio kwa uzuri." [5] Bwana Mungu
wa majeshi ndiye agusaye nchi na ikayeyuka; wote waishio humo wataomboleza;
yote yatainuka kama Mto, na itadidimia tena kama mto wa Misri. [6] Ni yeye ndiye
avijengaye vyumba vyake mbinguni, na kuanzisha kuba yake juu ya dunia. Yeye huita
maji ya bahari, na kuyamwaga juu ya uso wa dunia, Yahwe ndiye jina lake. [7] "Je ninyi
sio kama watu wa Kushi kwangu, wana wa Israeli? -hivi ndivyo Yahwe asemavyo.
Je sikuwapandisha Israeli kutoka nchi ya misri, Wafilisti kutoka Krete, na Washami
kutoka Kiri? [8] Tazama, macho ya Bwana Yahwe yako juu ya ufalme wenye dhambi,
na nitauharibu kutoka kwenye uso wa dunia, isipokuwa kwamba sintoiharibu
kabisa nyumba ya Yakobo -hivi ndivyo Yahwe asemavyo. [9] Tazama, nitaamuru, na
nitaipepeta nyumba ya Israeli miongoni mwa mataifa yote, kama mtu apepetaye
ngano kwenye ungo, hivyo basi hakuna hata chembe ya jiwe itakayoanguka kwenye
aridhi. [10] Watenda dhambi wote katika watu wangu watakufa kwa upanga, wale
wasemao, 'Majanga hayatatupita au kukutana nasi.' [11] Katika siku hiyo nitainua hema
ya Daudi iliyokuwa imeanguka, na kuyafunga matawi yake. Nitayainua magofu yake,
na kuijenga tena kama katika siku za zamani, [12] Kwamba wamiliki mabaki ya Edomu,
na mataifa yote ambayo yameitwa kwa jina langu -hivi ndivyo Yahwe asemavyo-
afanyayo haya. [13] Tazama, siku zitakuja-hivi ndivyo Yahwe asemavyo-wakati mlimaji
atampita mvunaji, na akanyagaye zabibu atampita yeye apandaye mbegu. Milima
itadondosha divai tamu, na milima yote itabubujika kwa nayo. [14] Nitawarudisha
kutoka utumwani watu wangu Israeli. Watajenga magofu ya miji na kuishi humo,
watapanda bustani za mizabibu na kunywa divai, na watafanya bustani na kula
matunda yao. [15] Nitaipanda hadi kwenye nchi yao, na hawataing'oa tena kutoka
kwenye nchi ambayo niliyowapatia," asema Yahwe Mungu wako.

# Obadia

1 Maono ya Obadia. Bwana MUNGU asema hivi juu ya Edomu Tumesikia habari
kutoka kwa Bwana, na mjumbe ametumwa kati ya mataifa, akisema, Inukeni!
Tuinuke dhidi yake kwa vita!” 2 Tazama, nitawafanya wadogo kati ya mataifa,
mutadharauliwa sana. 3 Kiburi cha moyo wako kimekudanganya wewe, wewe
ambaye unishi katika makaburi ya miamba, katika nyumba yako ya juu; asemaye
moyoni mwako, 'Ni nani atakayenishusha mimi chini?' 4 Ingawa unasimama juu
kama tai na ingawa kiota chako huwekwa kati ya nyota, nitakushusha chini kutoka
huko, asema Yahweh. 5 Kama wezi walikuja kwako, ikiwa wanyang'anyi wangekujilia
usiku (jinsi ungekatilwa mbali!), Wasingeweza kuiba vya kuwatosha? Ikiwa
wakusanya zabibu wangekujilia, wasingeacha mavuno? 6 Jinsi Esau amekwisha
kupigwa, na hazina zake zilizofichwa zimewekwa nje! 7 Watu wote wa ushirikiano
wako watakupeleka katika njiani ya hadi mpakani. Watu waliokuwa na amani
pamoja nawe wamekudanganya, na kukushinda. Wale wanaokula mkate wako
wameweka mtego chini yako. Hakuna uelewa ndani yake. 8 Je! Sikuweza siku
hiyo, asema Bwana, kuwaangamiza watu wenye hekima kutoka Edomu na kuelewa
kutoka mlima wa Esau? 9 Mashujaa wako watafadhaika, Temani, ili kila mtu akatiliwe
mbali kutoka mlima wa Esau kwa kuuawa. 10 Kwa sababu ya ukatili uliofanywa kwa
ndugu yako Yakobo, utafunikwa na aibu, nawe utakatiliwa mbali milele. 11 Siku
ile ulikuwa umesimama, siku wageni walichukua mali zake, na waliokuwa wageni
katika malango yake, na kupiga kura kwa Yerusalemu, wewe ulikuwa kama mmoja
wao. 12 Lakini usifurahi siku ya ndugu yako, siku ya msiba wake, wala usifurahi juu
ya watu wa Yuda siku ya uharibifu wao; msijisifu siku ya dhiki yao. 13 Usiingie mlango
wa watu wangu siku ya msiba wao; usifurahi juu ya taabu yao siku ya msiba wao,
wala msipotee utajiri wao siku ya uharibifu wao. 14 Usisimama kwenye njia panda,
ili kuwakatilia mbali wakimbizi wake na usiwatoe waathirika wake katika siku ya
dhiki. 15 Kwa maana siku ya Bwana iko karibu na mataifa yote. Kama ulivyofanya,
itafanyika kwako; matendo yako yatarudi juu ya kichwa chako mwenyewe. 16 Kwa
vile mlivyokunywa katika mlima wangu mtakatifu, ndivyo mataifa yote yatakavyo
kunywa daima. Watakunywa na kumeza na itakuwa kana kwamba hawakuwepo
kabisa. 17 Lakini katika Mlima Sayuni kutakuwa na wale waliookoka na watakuwa
watakatifu; na nyumba ya Yakobo watamiliki miliki zao. 18 Nyumba ya Yakobo
itakuwa moto, na nyumba ya Yusufu ni mwali wa moto, na nyumba ya Esau itakuwa
mabua makavu, nao watawaunguza, na kuwateketeza. Hakutakuwa na waathirika
kwa nyumba ya Esau, kwa kuwa Bwana amesema. 19 Wote kutoka Negebu watamiliki
mlima wa Esau na wale wa Shepela watamiliki nchi ya Wafilisti. Wao wataimiliki nchi
ya Efraimu na nchi ya Samaria; na Benyamini atamiliki Gileadi. 20 Wahamiaji wa jeshi
hili la watu wa Israeli watamiliki ardhi ya Kanaani mpaka Sarepta. Wahamiaji wa
Yerusalemu, waliopo Sefaradi, wataimiliki miji ya Negebu. 21 Waokoaji watakwenda
hadi juu ya Mlima Sayuni kutawala nchi ya vilima ya Esau, na ufalme utakuwa wa
Bwana.

# Yona

1 Ndipo neno la Bwana lilimjia Yona mwana wa Amittai, kusema, 2 “Simama uende
Ninawi, mji kuu, na ukapaze sauti dhidi yake, kwa sababu uovu wao umeinuka mbele
yangu.” 3 Lakini Yona akaondoka kukimbia kutoka mbele ya Bwana na kwenda
Tarshishi. Akatelemka mpaka Yafa na akaona melikebu inayokwenda Tarshishi. Kwa
hiyo alilipa nauli na akapanda melikebu kwenda nayo Tarishishi, mbali na uwepo
wa Yahweh. 4 Lakini Bwana akatuma upepo mkubwa juu ya bahari, ikawa tufani juu
ya bahari. Hivi karibuni ikaonekana kwamba meli ilikuwa inataka kuvunjika. 5 Wale
baharia waliogopa sana na kila mtu alilia kwa mungu wake mwenyewe. Wakatupa
mizigo bahari iliyokuwa merikebuni ili kuifungua. Yona alikuwa ameshuka hapa
pande za ndani ya melikebu, naye alikuwa amelala huko usingizi. 6 Basi nahoza
akamwendea akamwambia, “kwa nini unalala? Amka! ukamwombe mungu wako!
Labda mungu wako atatutambua na hatutapotea.” 7 Wote wakaambiana, 'Njoni,
tupige kura, ili tujue ni nani ndiye sababu ya mabaya haya yanayotupata.' Basi
wakapiga kura, na kura ikaangukia kwa Yona. 8 Kisha wakamwambia Yona,
“Tafadhali tuambie ni nani ndiye sababu ya mabaya haya yanayotupata. Unafanya
kazi gani, na umetoka wapi? Nchi yako ni ipi, na kutoka kwa watu wa kabila
gani?” 9 Yona akawaambia, Mimi ni Mhebrania; Nami namuogopa Bwana, Mungu
wa mbinguni, aliyeifanya bahari na nchi kavu. 10 Ndipo watu hao waliogopa zaidi,
wakamwambia Yona, Ni jambo gani hili ulilolifanya? Kwa maana hao watu walijua
kwamba alikuwa akikimbia mbele ya Bwana, kwa sababu alikuwa amewaambia.
11 Ndipo wakamwambia Yona, Tukufanyie nini ili bahari iweze kutulia? Kwa maana
bahari ilikuwa imechafuka zaidi na zaidi. 12 Yona akawaambia, “Nikamateni na
nitupeni baharini. Kisha bahari itatulia kwa ajili yenu, kwa maana najua kwamba
ni kwa sababu yangu kwamba tufani hii kubwa iwapate.” 13 Hata hivyo, watu
hao wavuta makasia kwa bidii ili kurudi nchi kavu, lakini hawakuweza kufanya
hivyo kwa sababu bahari ilikuwa imechafuka zaidi dhidi yao. 14 Basi wakamwomba
Bwana, wakasema, Tunakuomba, Bwana, tunakuomba, usiache tuangamize kwa
sababu ya maisha ya mtu huyu; wala usituwekee hatia ya kufa kwake, kwa kuwa
wewe, Bwana, umefanya kama ulivyopenda. 15 Basi wakamchukua Yona wakamtupa
baharini, nayo bahari ikaacha kuchafuka. 16 Ndipo watu wale wakamuogopa Bwana
sana. Wakamtolea dhabihu Bwana na kuweka nadhiri. 17 Bwana alikuwa ameandaa
samaki mkubwa kummeza Yona, na Yona alikuwa ndani ya tumbo lasamaki siku tatu
na usiku wa tatu.

## 2

1 Kisha Yona akamwomba Bwana Mungu wake kutoka katika tumbo la samaki.
2 Akasema, Nimemwita Bwana juu ya shida yangu naye akanijibu; kutoka tumbo
la Kuzimu nililia kwa msaada! Uliisikia sauti yangu. 3 Ulikuwa umenitupa ndani
ya kina, ndani ya moyo wa bahari, na maji yaliyonizunguka; mawimbi yako yote
na gharika yalipita juu yangu. 4 Nikasema, 'Nimefukuzwa mbele ya macho yako;
lakini nitaangalia tena juu ya hekalu lako takatifu. ' 5 Maji yalifunika kunizunguka
karibu na shingo yangu; kina kilinizunguka; mwani ukakizinga kichwa changu.
6 Nilikwenda chini ya milima; nchi na baa zake zimefungwa juu yangu milele. Lakini
wewe umeinua uhai wangu shimoni, Bwana, Mungu wangu! 7 Wakati nafsi yangu
ilipozimia ndani yangu, nikamwita Bwana; basi sala yangu ilikujia, katika hekalu
lako takatifu. 8 Wote ambao huzingatia miungu isiyofaa hukataa uaminifu wako
wao wenyewe. 9 Lakini mimi, nitakuchinjia kwa sauti ya shukrani; Nitayatimiza

yale niliyoapa. Wokovu hutoka kwa Bwana! [10] Kisha Bwana akanena na samaki,
akamtapika Yona juu ya nchi kavu.

# 3

[1] Neno la Bwana likamjia Yona mara ya pili, akisema, [2] "Ondoka, uende Ninawi,
mji ule mkubwa, na uhubiri ujumbe ule ambao nitakuagiza." [3] Basi Yona akaondoka
akaenda Niniawi kwa kutii neno la Bwana. Sasa Ninawi ilikuwa mji mkubwa sana,
ilikuwa safari ya siku tatu. [4] Yona akaanza kuingia ndani ya mji, na baada ya safari
ya siku, akapaza sauti, akasema, "Katika siku arobaini Ninawi itaangamizwa." [5] Watu
wa Ninawi walimwamini Mungu na wakatangaza kufunga. Wote hwakavaa nguo za
magunia, kutoka aliyemkubwa hata mdogo. [6] Mapema habari zilimfikia mfalme wa
Ninawi. Akasimama kutoka kiti chake cha enzi, akavua vazi lake, akajivika magunia,
akaketi katika majivu. [7] Alitoa tangazo ambalo lilsemalo, "katika mji wa Ninawi,
kwa mamlaka ya mfalme na wakuu wake, msiruhusu mtu wala mnyama, ng'ombe
wala kundi, asionje kitu chochote. Wao wasile wala kunywe maji. [8] Lakini watu na
wanyama wawe wamefunikwa kwa magunia na walie kwa sauti kubwa kwa Mungu.
Kila mtu ageuke na kuacha njia yake mbaya na kutoka katika udhalimu uliyopo
mikononi mwake. [9] Nani anajua? Mungu anaweza kurejea na kubadili mawazo yake
na kuacha ghadhabu yake kali ili tusiangamie." [10] Mungu akaona yale waliyoyafanya,
wakaziacha njia zao mbaya. Kwa hiyo Mungu alibadili mawazo yake juu ya adhabu
aliyowaambia angewafanyia, nae hakufanya hivyo.

# 4

[1] Lakini hili lilimchukiza Yona naye akakasirika. [2] Basi Yona akamwomba Bwana
akasema, "Ee, Bwana, hiya sio yale niliyosema wakati niliporudi katika nchi yangu?
Ndiyo maana nilifanya haraka na kujaribu kukimbia Tarshishi-kwa sababu nilijua
kuwa wewe ni Mungu mwenye neema, mwenye huruma, si meingi wa hasira, mwingi
kwa uaminifu, na hughairi maafa. [3] Kwa hiyo sasa, Bwana, nakuomba, uniondoe
uhai wangu, kwa maana ni bora kwangu kufa kuliko kuishi." [4] Bwana akasema, Je,
ni vema kwamba umekasirika?" [5] Kisha Yona akaondoka mjini akaketi upande wa
mashariki wa jiji. Huko alifanya makao na akaketi chini yake katika kivuli ili aweze
kuona mji utakuwaje. [6] Bwana Mungu aliandaa mmea na kuukuza juu ya Yona ili uwe
kivuli juu ya kichwa chake ili kupunguza dhiki yake. Yona alikuwa na furaha kubwa
kwa sababu ya mmea. [7] Lakini Mungu aliandaa mdudu kulipopambazuka asubuhi
iliyofuata. Alishambulia mmea na mmea ukapooza. [8] Ikawa wakati jua lilipochomoza
asubuhi, Mungu aliandaa upepo mkali wa mashariki. Pia, jua lilipiga kichwa cha
Yona na akaanguka. Kisha Yona alitamani kufa. Akajiambia, "Ni bora kwangu kufa
kuliko kuishi." [9] Kisha Mungu akamwambia Yona, "Je, ni vema wewe kuwa na hasira
juu ya mmea?" Yona akasema, Ni vyema kuwa nimekasirika hata kufa. [10] Bwana
akasema, Umeuhurumia mmea, ambao haukuufanyia kazi wala haukukua. Uliomea
katika usiku na kufa usiku. [11] Kwa hiyo mimi, haikunipassa kuuhurumia Ninawi, mji
mkuu, ambalo kuna watu zaidi ya mia na ishirini elfu ambao hawajui tofauti kati ya
mkono wao wa kulia na mkono wao wa kushoto, na pia ng'ombe wengi?

# Mika

1 Hili ni neno la Yahwe ambalo lilikuja kwa Mika Mmorashti katika siku za
Yotahamu, Ahazi, na Hezekeia, mfalme wa Yuda, lile neno aliloliona kuhusiana na
Samaria na Yerusalemu. 2 Sikilizeni, ninyi watu wote. Sikilizeni, dunia, na vyote
vilivyomo kwenye dunia. Acheni Yahwe ashuhudiwe dhidi yenu, Bwana kutoka
kwenye hekalu lake takatifu. 3 Tazama, Yahwe anakuja kutoka mahali pake; atashuka
chini na kupakanyaga mahali pa juu katika dunia. 4 Milima itayeyuka chini yake;
mabonde yatapasuka vipande vipande kama mshumaa mbele ya moto, kama maji
ambayo yamemwagika chini ya mteremko mkali. 5 Haya yote ni kwasababu ya uasi
wa Yakobo, na kwasababu ya dhambi za nyumba ya Israeli. Je sababu ilikuwa nini
kwa uasi wa Yakobo? Je ilikuwa Samaria? Je sababu ilikuwa nini kwa mahali pa
juu pa Yuda? Je haiukuwa Yerusalemu? 6 “Nitaifanya Samaria rundo la uharibifu
katika shamba, kama eneo la kupandia mizabibu. Nitayavuta mawe ya jengo lake
kwenda kwenye bonde; Nitaifunua misingi yake. 7 Sanamu zake zote za kuchonga
zitapondwa vipande vipande; na zawadi zake zote zitachomwa moto. Kwa kuwa
zawadi zake za ukahaba amezikusanya, na kama malipo ya ukahaba yatarudi.” 8 Kwa
sababu hii nitalia na kuomboleza; nitaenda peku peku na uchi; Nitaomboleza kama
mbeha na kuomboleza kama bundi. 9 Kwa kuwa jeraha lake haliponi, kwa kuwa
imefika kwa Yuda. Imefikia lango la watu wangu, hadi Yerusalemu. 10 Msiache
kuwambia kuhusu katika Gathi; msilie tena. Katika Bethi Leafra nabiringisha
mwenyewe kwenye mavumbi. 11 Piteni karibu na, makao ya Shafiri, katika uchi
na aibu. Makazi ya Zaanani hayatatoka nje. Maombolezo ya Beth Ezeli, kwa ajili
ya ulinzi yamechukuliwa. 12 Kwa kuwa wakaaji wa Marothi hungoja habari njema,
kwa sababu hofu, kwa sababu msiba umetoka kwa Yahwe hadi kwenye malango ya
Yerusalemu. 13 Wfuungeni lijamu farasi wakokote gari la farasi, makazi ya Lakishi.
Wewe Lakishi, ulikuwa mwanzo wa dhambi kwa binti Sayuni, kwa kuwa makosa ya
Israeli yalionekana kwako. 14 Hivyo utaipa zawadi ya kuagia Moreshethi Gathi; mji
wa Akzibu utawavunja moyo wafalme wa Israeli. 15 Tena nitaleta ushindi kwako,
makazi ya Maresha; uzuri wa Israeli utakuja Adulamu. 16 Kata kipara chako na
kata nywele zako kwa ajili ya watoto ambao unaowafurahisha. Fanya kipara chako
mwenyewe kama tai, kwa ajili ya watoto wako watakao kwenda utumwani kutoka
kwako

# 2

1 Ole wao wale wanao wanaokusudia mabaya, kwa wale wanaokusudia kwenye
vitanda vyao kufanya maovu. Katika asubuhi wanayafanya kwa sababu wana nguvu.
2 Wanatamani mashamba na kuyapunguza; wanazitamani nyumba na kuzichukua.
Wanadhulumu mtu na nyumba yake, mtu na urithi wake. 3 Kwa hiyo Yahwe asema
hivi, “Tazama, nakaribia kuleta janga dhidi ya huu ukoo, ambalo hamtazitoa shingo
zenu. Hamtatembea kwa kiburi, kwa kuwa itakuwa wakati wa uovu. 4 Katika siku
hiyo maadui zako wataimba wimbo kuhusu wewe, na kuomboleza kwa maombolezo
ya huzuni. Wataimba, 'Sisi Waisraeli tumeangamizwa kabisa; Yahwe hubadilisha
eneo la watu wangu. Je ataliondoaje kutoka kwangu? Huwagawia mshamba yetu
kusaliti.”' 5 Kwa hiyo, ninyi watu matajiri hamtakuwa uzao kugawanya eneo kwa
kupiga kura katika mkutano wa Yahwe. 6 “Msitabiri,” wanasema. “Hawatayatabiri
haya mambo; lawama hazitakuja.” 7 Je litasemwa kweli, nyumba ya Yakobo, “je
Roho ya Yahwe? Je haya ni matendo yake kweli?” Maneno yangu hayafai kwa kila
mmoja atembeaye kwa unyoofu? 8 Hivi karibuni watu wangu wameinuka kama adui.

Mmelivua joho, nguo, kutoka wale wapitao wasioshutumiwa, kama maaskari kurudi
kutoka kwenye vita kwa kile wakifikiriacho ni salama. [9] Mnawaendesha wanawake
wangu kwa watu wangu kutoka kwenye nyumba nzuri; mnachukua baraka kutoka
kwa watoto wao wadogo daima. [10] Inukeni na muondoke, kwa kuwa hii sio
sehemu ambayo mnaweza kuishi, kwa sababu ya unajisi wake; imeangamizwa kwa
maangamizo kabisa. [11] Kama mtu akija kwenu katika roho ya uongo na kudanganya
na kusema, “Nitatabiri kwenu kuhusu mvinyo na kilevi kikali,” angeweza kufikiriwa
kuwa nabii kwa ajili ya hawa watu. [12] Nitawaleta pamoja wote hakika, Yakobo.
Hakika nitawakusanya mabaki ya Israeli. Nitawaleta pamoja kama kondoo katika
zizi, kama kundi la wanyama katika malisho. Kutakuwa na kelele kwasababu ya
wingi wa watu. [13] Mtu avunjaye hufungua njia zao kwa ajili yao kwenda mbele yao.
Wamebomoa kupitia lango na kutoka nje; mfalme wao atapita mbele yao. Yahwe
atakuwa mbele yao.

# 3

[1] Nimesema'”Sasa sikilizeni, ninyi viongozi wa Yakobo na kutawala nyumba ya
Israeli: Je siyo sahihi kwenu kuielewa haki? [2] Ninyi manaochukia mazuri na kupenda
uovu, ninyi mnaoambua ngozi yao, miili yao kutoka kwenye mifupa yao- [3] ninyi
mnaokula pia miili ya watu wangu, na kuambua ngozi yao, kuvunja mifupa yao, na
kuwakatakata katika vipande vipande, kama nyama kwenye chungu, kama nyama
kwenye sufuria kubwa. [4] Kisha ninyi watawala mtalia kwa Yahwe, lakini hatawajibu.
Atauficha uso wake kutoka kwenu kipindi hicho, kwasababu mmefanya matendo
maovu.” [5] Yahwe asema hivi kuhusu manabii ambao wawafanyao watu wangu
kushindwa, “Kwa wale wawalishao wanatangaza, 'Kutakuwa na ustawi.' Lakini kwa
wale wasioweka kitu kwenye vinywa vyao, wanaanzisha vita dhidi yake. [6] Kwa
hiyo, itakuwa usiku kwenu usiokuwa na maono juu yenu; itakuwa giza ili kwamba
msiweze kubashiri. Jua litakwenda chini juu ya manabii, na siku itakuwa giza
juu yao. [7] Waonaji watawekwa kwenye aibu, waaguzi wa watachanganyikiwa.
Wote watafunga midomo yao, kwa kuwa hakuna jibu kutoka kwangu.” [8] Lakini
kwangu, nimejazwa nguvu kutoka kwa Roho wa Yahwe, na nimejaa haki na uweza,
kumwambia Yakobo kosa lake, na Israeli dhambi yake. [9] Sasa sikieni hii, ninyi
viongozi wa nyumba ya Yakobo, na watawala wa nyumba ya Israeli, ninyi ambao
mnaochukia haki, na kupotosha kila haki. [10] Mnaijenga Sayuni kwa damu na
Yerusalemu kwa uovu. [11] Viongozi wenu huhukumu kwa rushwa, makuhani wenu
hufundisha kwa hijara, na manabii wenu hufanya utabiri kwa ajili ya pesa. Hata
hivyo bado mtamtegemea Yahwe na kusema, “Je hayupo Yahwe pamoja nasi? Hakuna
uovu utakaokuja juu yetu.” [12] Kwa hiyo, kwasababu yenu, Sayuni italimwa kama
shamba, Yerusalemu itakuwa rundo la kifusi, na mwinuko wa hekalu utakuwa kama
mwinuko wa msituni.

# 4

[1] Lakini katika siku za mwisho itakuja kuhusu kwamba mlima wa nyumba ya
Yahwe utawekwa imare juu ya milima mingine. Utainuliwa juu ya milima, na
watu watautakabisha. [2] Mataifa mengi yataenda na kusema, “Njoni, twendeni juu
kwenye mlima wa Yahwe, kwenye nyumba ya Mungu wa Yakobo. Atatufundisha
njia zake, na tutembea katika njia zake.” Kwa kuwa kutoka Sayuni sheria itatoka,
na neno la Yahwe kutoka Yerusalemu. [3] Atahukumu miongoni mwa watu na
kuamua kuhusiana na mataifa mengi ya mbali. Watapoga mapanga yao kuwa
plau na mikuki yao kuwa miuundu ya kupogolea. Taifa halitainua upanga dhidi
ya taifa, wala kutawala kwa vita tena. [4] Badala yake, wataketi kila mtu chini ya

mzabibu wake na chini ya mtini wake. Hakuna mtu atakayewafanya waogope,
kwa kuwa mdomo wa Yahwe wa majeshi umesema. [5] Kwa kuwa watu wote
wataenenda, kila mmoja, katika jina la mungu wake. Lakini sisi tutaenenda
katika jina la Yahwe Mungu wetu milele na milele. [6] “Katika siku hiyo,” aseme
Yahwe, “Nitamkusanya achechemeaye na kumkusanya aliyefukuzwa, wale ambao
nimewatesa. [7] Nitamrudisha aliyechechemea kwenye mabaki, na yeye aliyetupwa
kwenye taifa imara, na mimi, Yahwe, nitatawala juu yao katika Milima Sayuni,
sasa na milele. [8] Kama kwako, mnara wa saa kwa ajili ya kundi, mlima wa binti
wa Sayuni-utakuja kwenu, utawala wenu wa zamani utarudishwa, ufalme ambao
unaomilikiwa na binti wa Yerusalemu. [9] Sasa, kwa nini unapiga kelele kwa sauti
kuu? Je hakuna mfalme miongoni mwenu? Je mshauri wako amekufa? Kwa nini
uchungu umekushika kama yule mwanamke akiwa anazaa? [10] Kuwa katika uchungu
wa kuzaa ili uzae, binti Sayuni, kama mwanamke mwenye uchungu. Kwa sasa
utatoka nje ya mji, kuishi kwenye shamba, na kwenda Babeli. Huko utaokolewa.
Huko Yahwe atakuokoa kutoka kwenye mikono ya maadui. [11] Sasa mataifa mengi
yamekusanyika juu yako; wakisema; 'Atiwe unajisi; macho yenu yaangalie Sayuni.”'
[12] Nabii asema, “Hawayajui mawazo ya Yahwe, wala hawaelewi mpango wake,
kwa kuwa wamewakusanaya kama miganda kupura sakafuni.” [13] Yahwe asema,
“siamama na upure, binti Sayuni, kwa kuwa nitaifanya pembe yako kuwa chuma,
na nitazifanya kwato zako kuwa shaba. Utaponda watu wengi. Nitaweka wakfu
udhalimu wao kwangu mwenyewe, Yahwe, miliki zao kwangu, Bwana wa dunia
nzima.”

# 5

[1] Sasa njoni pamoja katika safu ya kupigana, binti wa maaskari; maaskari
wameuzingira mji, kwa ufito watampiga mwamuzi wa Israeli kwenye shavu. [2] Lakini
wewe, Bethlehemu Efrata, hata kama uko mdogo miongoni mwa koo za Yuda, kutoka
kweko mmoja atakuja kwangu kutawala Israeli, ambaye mwanzo wake ni kutoka
nyakati za kale, toka milele. [3] Kwa hiyo Mungu atawapa, hata mda wa yeye aliye
katika uchungu kuzaa mtoto, na mabaki ya ndugu zake yatawarudia wana wa
Israeli. [4] Atasimama na kuchunga kundi lake kwa nguvu za Yahwe, kwa ukuu
wa enzi ya jina la Yahwe Mungu wake. Watabaki, kwa kuwa atakuwa mashuhuri
hata mwisho wa dunia. [5] Atakuwa amani yetu. Wakati Waashuru watakapokuja
kwenye nchi yetu, wakati wakitembea dhidi ya boma yetu, kisha kisha tutainuka
juu yao wachungaji saba na viongozi nane juu ya watu. [6] Watachunga nchi ya
Ashuru kwa upanga, na nchi ya Nimrodi katika malango yake. Atatuokoa kutoka kwa
Waashuru, watakapokuja kwenye nchi yetu, watakapoingia kwenye mipaka yetu.
[7] Mabaki ya Yakobo yatakuwa katika kabila za watu wengi, kama umande utokao kwa
Yahwe, kama manyunyu kwenye majani, ambayo hayamsubiri mtu, na hayawasubiri
watoto wa mwanadamu. [8] Mabaki ya Yakobo yatakuwa miongoni mwa mataifa,
miongoni mwa watu wengi, kama simba katikati ya kundi la kondoo. wakati akipita
katikati yao, atawakanyaga juu yao na kuwachachana kuwa vipande vipande, na
hakutakuwa na mtu wa kuwaokoa. [9] Mkono wako utainuliwa dhidi ya maadui zako,
na utawaharibu. [10] “Itatokea siku hiyo,” asema Yahwe, “kwamba nitawaharibu farasi
wako kutoka miongoni mwenu na nitayavunja magari yako ya farasi. [11] Nitaiharibu
miji katika nchi yako na kuzingusha ngome zako zote. [12] Nitauharibu uchawi kwenye
mkono wako, na hakutakuwa na waaguzi tena. [13] Nitaziaharibu sanamu zako za
pango na nguzo za mawe kutoka miongoni mwako. Hautaabudu tena ustadi wa
mikono yako. [14] Nitazin'goa nguzo zako za Ashera kutoka miongoni mwenu, na

nitaiharibu miji yenu. 15 Nitalipiza kisasi kwa hasira na ghadhabu juu ya mataifa
ambayo hayakusikiliza."

## 6

1 Sasa sikilizeni kile ambacho Yahwe asemacho, "Inuka na ueleze kesi yako mbele
ya milima; acha milima isikie sauti yako. 2 Sikilizeni madai ya Yahwe, enyi milima,
na ninyi misingi mivumilivu ya dunia. Kwa kuwa Yahwe anavumilia pamoja na watu
wake, na atapigana katika mahakama juu ya Israeli." 3 Watu wangu, nimefanya nini
kwenu? nimewachosha mara ngapi? shuhudieni dhidi yangu! 4 Kwa kuwa niliwaleta
kutoka nchi ya Msiri na kuwaokoa kutoka kwenye nyumba ya utumwa. Nawatuma
Musa, Aruni, na Mariamu kwako. 5 Watu wangu, kumbukeni ambavyo Balaki mfalme
wa Moabu alivyotunga, na vile ambavyo Balamu mwana wa Beori alivyomjibu kama
ulipokuwa ukienda kutoka kwa Gilgali, hivyo mnaweza kujua matendo ya haki ya
Yahwe." 6 Je nilete nini kwa Yahwe, ninapoenda kumwinamia Mungu aliye juu? Je
ninaweza kuja kwake na sadaka za kuteketeza, pamoja na ndama wenye mwaka
mmoja? 7 Je Yahwe atapendezwa na maelfu ya kondoo waume, au na elfu kumi
za mito ya mafuta? Je nimtoe mzaliwa wangu wa kwanza kwa ajili ya kosa langu,
tunda la mwili wangu kwa ajili ya dhambi yangu mwenyewe? 8 Amekwambia,
mtu, kile kilicho bora, na kile ambacho Yahwe atakacho kutoka kwako: Kutenda
haki, kupenda ukarimu, na kutembea kwa unyenyekevu pamoja na Mungu wako.
9 Sauti ya Yahwe inatangaza kwenye mji-hata sasa hekima hukukiri jina lako: "Kaa
tayari kwa ajili ya fimbo, na kwa yule aliyeiweka. 10 Kuna utajiri katika nyumba
za waovu, na kipimo cha uongo hilo ni chukizo mno. 11 Ningeweza kumfikira
mtu kuwa hana hatia kama anatumia kipimo cha ulaghai, pamoja na mfuko wa
kipimo wa udanganyifu? 12 Matajiri wamejaa uharibifu, makazi yao yamesema
uongo, na ulimi wao katika midomo yao unaudanganyifu. 13 Kwa hiyo nimekupiga
kwa pigo linaloumiza, nimekufanya gofu kwa sababu ya dhambi zako. 14 Utakula
lakini hutatosheka; utupu wako utabakia ndani yako. Utatunza mizigo mbali lakini
hutahifadhi, na kile unachokihifadhi nitakitoa kwa upanga. 15 Utapanda lakini
huatavuna; utazikusanya zaituni lakini hutajipaka mafuta; utasindika zabibu lakini
hutakunywa divai. 16 Kanuni zilizotengenezwa na Omri zimetunzwa, na matendo
yote ya nyumba ya Ahabu. Mnatembea kwa ushauri wao. Hivyo nitakufanya wewe,
mji, gofu, na makazi yako jambo la zomeo, na matabeba dharau kama watu wangu."

## 7

1 Ole wangu! Kwangu mimi ni kama msimu wa mavuno ulipokwisha, na
pia makombo ya mavuno ya zabibu kwenye shamba la mizabibu: Hakuna tena
kishamba cha matunda kinachoonekana, hakuna matini ya malimbuka ambayo
ninayoyatamani. 2 Watu waaminifu wamepotelea kutoka kwenye nchi, hakuna mtu
mwadilifu katika wanadamu wote. Wote hudanganya katika kusubiri kumwaga
damu; kila mtu humuwinda ndugu yake mwenyewe kwa wavu. 3 Mikono yao
ni mizuri mno kwa kufanya madhara. watawala huuliza pesa, hakimu yuko
tayari kwa rushwa, na mtu mwenye nguvu anawaambia wengine kile anachokitaka
kujipatia. Hivyo ndivyo waundavyo kwa pamoja. 4 Mtu bora kwao ni kama
mitemba, mwadilifu sana ni kama mche wa miba. Imefika siku iliyosemwa nyuma
na walinzi wako, siku ya hukumu. Sasa ni mda wa machafuko. 5 Msimwamini
kila jirani; msimuweke kiongozi katika rafiki yeyote. Kuweni makini kuhusiana
na kile msemacho hata kwa mwanamke ambaye adanganyaye kwenye mikono
yenu. 6 Kwa kuwa mwana humfedhehesha baba yake, binti huinuka kushindana
na mama yake, na mke wa mwana wa kiume hushindana na mama mkwe wake.

Adui wa watu ni watu wa nyumba yake mwenyewe. 7 Lakini kama kwangu
mimi, nitamtazama Yahwe. Nitamsubiri Mungu wa wokovu wangu; Mungu wangu
ataniskia. 8 Usifurahi juu yangu, adui yangu. Niangukapo, nitainuka. Wakati
nitakapokuwa nimekaa katika giza, Yahwe atakuwa mwanga kwangu. 9 Kwasababu
nimetenda dhambi dhidi ya Yahwe, nitachukua ghadhabu yake hata aniteteapo
kosa langu, na kutekeleza hukumu kwa ajili yangu. Atanileta kwenye nuru, na
nitamwona akiniokoa kwenye haki yake. 10 Kisha adui yangu atakapoliona hilo,
na aibu itamfunika yule aliyeniambia, “Yahwe Mungu wako yuko wapi?” macho
yangu yatamtazama; atakanyagwa chini kama tope kwenye mitaa. 11 Siku ya ya
kujenga kuta zako zitafika; siku hiyo mipaka itasogezwa mbali sana. 12 Siku hiyo watu
watakuja kwako, kutoka Ashuru na miji katika Misri, kutoka Misri hata mto mkubwa,
kutoka bahari kwenda bahari, na kutoka mlima kwenda mlima. 13 Hizo nchi zitakuwa
zimejitenga kwasababu ya watu ambao wanaishi huko sasa, kwasababu ya tunda
la matendo yao. 14 Chunga watu wako kwa fimbo yako, kundi la urithi wako.
Wanaishi wenyewe kwenye msitu, katikati ya msitu. Wachunge katika Bashani na
Gileadi kama siku za zamani. 15 Kama katika siku wakati mlipotoka nje ya nchi ya
Misri, nitawaonyesha maajabu. 16 Mataifa yataona na kuwa na aibu ya nguvu zao
zote. Wataweka mikono yao kwenye midomo yao; masikio yao yatakuwa kiziwi.
17 Watalamba vumbi kama nyoka, kama viumbe vitaambavyo juu ya nchi. Watatoka
nje kwenye maficho kwa hofu; watakuja kwako kwa hofu, Yahwe Mungu wetu, na
wataogopa kwa sababu yako. 18 Ni nani aliye Mungu kama wewe, wewe uchukuaye
dhambi, wewe upitaye juu ya kosa la mabaki ya mrithi wako? Hutunzi hasira yako
milele, kwa sababu unapenda kutuonyesha agano lako la aminifu. 19 Tena utakuwa
na huruma juu yetu; utayakanyaga maovu chini ya miguu yako. Utazitupa dhambi
zetu zote kwenye vilindi vya bahari. 20 Utampatia ukweli Yakobo na agano aminifu
kwa Abrahamu, ulipoapa kwa babu zetu katika siku za kale.

# Nahumu

[1] Maono kuhusu Ninawi. Kitabu cha maono ya Nahumu, Mwelkoshi. [2] Yehova ni
Mungu mwenye wivu na analipa kisasi; Yehova hulipa kisasi na amejaa ghadhabu;
Yohova analipiza kisasi kwa adui zake, na huiendeleza hasira yake kwa adui zake.
[3] Yehova ni mwenye nguvu nyingi na mpole wa hasira; hatakuwa na namna ya
kuacha kuwahesabia hatia adui zake. Yehova hufanya njia yake kwenye upepo wa
kisulisuli na dhoruba, na mawingu ni mavumbi ya miguu yake. [4] Huikemea bahari
na kuifanya ikauke; hukausha mito yote. Bashani ni dhaifu, na Karmeli pia; maua
ya Lebanoni ni dhaifu. [5] Milima hutetema kwenye uwepo wake, na vilima huyeyuka;
dunia huanguka mbele zake, kabisa, dunia na watu wote wanaoishi ndani yake.
[6] Ni nani anaweza kusimama mbele ya ghadhabu yake? Nani anaweza kuzuia ukali
wa hasira yake? Ghadhabu yake imemwagwa kama moto, na miamba ameibomoa
mbalimbali. [7] Yehova ni mwema, boma katika siku ya taabu; na yeye ni mwaminifu
kwa wale wanaomkimbilia. [8] Lakini atafanya mwisho wa adui zake kwa mafuriko
ya kutisha; atawawinda kwenye giza. [9] Watu wanapanga nini dhidi ya Yehova? Yeye
atakomesha; taabu haitainuka mara ya pili. [10] Maana watakuwa wamevurugika
kama michongoma; wataloweshwa katika kinywaji chao mwenyewe; wataharibiwa
kabisa kwa moto kama mashina ya mabua. [11] Mtu mmoja aliinuka miongoni mwenu,
Ninawi, aliyepanga ubaya dhidi ya Yehova, mtu ambaye aliimarisha uovu. [12] Hivi
ndivyo anavyosema Yehova, “Hata kama wananguvu zao timilifu na idadi timilifu,
hata hivyo watanyolewa, watu wao hawatakuwepo tena. Bali wewe, Yuda: Ingawa
nimekutesa, sitakutesa tena. [13] Sasa nitaivunja ile nira ya watu kutoka kwako;
nitaikata minyororo yako. [14] Yehova ametoa amri juu yako, Ninawi: “ Hakutakuwa na
kizazi tena chenye kubeba jina lako. Nitazizuia sanamu zilizochongwa na kuziondoa
sanamu za chuma kutoka kwenye nyumba za miungu yenu. Nitachimba makaburi
yenu, kwa kudharauliwa kwenu.” [15] Tazama, juu ya milima kuna miguu ya mtu
aletaye habari njema, anayetangaza amani! Sherehekeeni sikukuu zenu, Yuda, na
tunzeni nadhiri zenu, kwa maana mwovu hatawavamia tena; ameondolewa kabisa.

## 2

[1] Yule ambaye atakuharibu vipande vipande anakuja dhidi yako. Linda kuta
za mji, linda barabara, jitieni nguvu ninyi wenyewe, yakusanyeni majeshi yenu.
[2] Maana Yehova anarejesha fahari ya Yakobo, kama fahari ya Israeli, ingawa wateka
nyara waliwaharibu na kuharibu matawi ya zabibu zao. [3] Ngao za mashujaa
wake ni nyekundu, na watu hodari wamevaa nguo nyekundu; magari ya vita
yameandaliwa yanang'ara kwenye vyuma vyake wakati wa mchana, na mikuki ya
mivinje inarushwa hewani. [4] Magari ya vita yapo kasi kwenye mitaa; yanakimbia
mbele na nyuma katika mitaa. Yapo kama kurunzi, na yanakimbia kama radi.
[5] Yule ambaye atakuvunja vipande vipande anawaita maafisa wake; wanajikwaa
kila mmoja kwa mwingine katika kutembea kwao; wanaharakisha kuushambulia
ukuta wa mji. Ngao kubwa imetayarishwa kujikinga na hawa washambuliaji.
[6] Malango kwenye mito yamelazishwa kufunguka, na jumba la mfalme linaanguka
kwenye uharibifu. [7] Husabu amevuliwa mavazi yake na amachukuliwa; watumishi
wake wa kike wanaomboleza kama njiwa, wanavipiga vifua vyao. [8] Ninawi ni
kama bwawa la maji linalovuja, watu wake kwa pamoja wanakimbia kama maji
yanayotiririka. Wengine wanasema, “ Simama, simama,” lakini hakuna anayegeuka
nyuma. [9] Chukua nyara ya fedha, kuchua nyara ya dhahabu, maana hakuna mwisho

wake, kwa fahari ya vitu vyote vizuri vya Ninawi. 10 Ninawi ipo tupu na imeharibiwa.
Moyo wa kila mtu unayeyuka, magoti ya kila mmoja yanagongana pamoja, na
uchungu upo kwa kila mmoja; sura zao wote zimepauka. 11 Sasa liko wapi pango
la simba, sehemu ambapo simba wadogo hula chakula, sehemu ambapo simba
dume na simba jike walitembea, pamoja wana-simba, ambapo hawakuogopa kitu
chochote? 12 Simba alirarua mawindo yake vipande vipande kwa ajili ya watoto
wake; aliwanyonga mawindo wake kwa ajili ya wake zake, na kulijaza pango lake
mawindo, makao yake kwa mizoga iliyoraruliwa. 13 "Tazama, mimi nipo kinyume
na wewe- hili ni neno la Yehova wa majeshi. Nitayachoma magari yenu ya vita
katika moshi, na upanga utateketeza simba wenu vijana. Nitazuia nyara zenu kutoka
kwenye nchi yangu, na sauti za wajumbe wenu hazitasikika tena."

# 3

1 Ole kwa mji uliojaa damu! Wote umejaa uongo na mali za wizi; wahanga
wapo kwake daima. 2 Lakini sasa kunasauti ya mijeledi na sauti za kugongesha
matairi, farasi wakicheza, na magari ya vita yanaruka ruka. 3 Kuna wapanda
farasi wanashambulia, Upanga unang'ara, mikuki inametameta, marundo ya maiti,
mafungu makubwa ya miili; hakuna ukomo wa miili, washambuliaji wanajikwaa juu
yake. 4 Hii inatokea kwa sababu ya matendo ya tamaa ya kahaba mzuri, mzoefu wa
uchawi, mwenye kuuza taifa kwa umalaya wake, na watu kwa njia ya matendo yake
ya kichawi. 5 " Tazama, mimi nipo kinyume na wewe- hili ni neno la Yehova wa
majeshi- sketi yako nitaiinua juu ya uso wako na kuzionyesha sehemu zako za siri
kwa mataifa, aibu yako kwa falme. 6 Nitarusha uchafu wa kuchukiza na kukufanya
uwe mbaya sana; nitakufanya uwe mtu wa kutazamwa na kila mmoja. 7 Itakuwa
kwamba kila mmoja anayekutazama atakukimbia na kusema, " Ninawi ameharibika;
ni nani ataomboleza kwa ajili yake?' Ni wapi nitampata mtu anayeweza kukufariji?"
8 Ninawi, je wewe ni bora kuliko Noamoni, uliojengwa juu ya Mto Naili, uliokuwa
umezungukwa na maji, ambao ulinzi wake ilikuwa bahari, ambao ukuta wake
ilikuwa bahari yenyewe? 9 Ethiopia na Misri zilikuwa nguvu zake, na mwisho wake
haukuwepo; Putu na Libya walikuwa rafiki zake. 10 Lakini Noamoni alichukuliwa;
alikwenda kwenye mateka; watoto wake wadogo walivunjwa vipande vipande katika
kila makao makuu ya mtaa; adui zake walipiga kura kwa watu wake wenye heshima
na wakuu wake wote walifungwa minyororo. 11 Wewe pia utalewa; utajaribu
kujificha, na utatafuta makimbilio kutoka kwa adui yako. 12 Ngome zako zote
zitakuwa kama mitini yenye tini zilizoiva mapema: kama zikitikiswa, zitaangukia
kwenye kimywa cha mlaji. 13 Tazama, watu miongoni mwenu ni wanawake; malango
ya nchi yako yamefunguliwa sana kwa ajili ya adui zako; moto umeharibu bawaba
zake. 14 Nenda ukachote maji kwenye boma iliyozingirwa; ziimarishe ngome zako;
nenda kwenye udongo na kandamiza matope; finyanga kwa ajili ya matofali. 15 Moto
utakuteketeza pale, na upanga utakuangamiza. Utateketezwa kama nzige wachanga
wanavyoteketeza kila kitu. Ninyi wenyewe mjitengeneze kuwa wengi kama nzige
wachanga, na wengi kama nzinge waliopevuka. 16 Umezidisha wafanyabiashara
wako zaidi kuliko nyota mbinguni; lakini wapo kama tunutu: wanapora nchi na kisha
kuruka kwenda mbali. 17 Wafalme wenu wapo wengi kama zinge, na wakuu wenu
wa majeshi ni kama kundi la wadudu wenye kuweka kambi katika ukuta wakati wa
baridi. Lakini jua linapowaka wanaruka kwenda mbali ambako hakuna anayepajua.
18 Mfalme wa Ashuru, wachungaji wako wamelala; watawala wako wamejilaza chini
kupumzika. Watu wako wametawanyika juu ya milima, na hakuna hata mmoja
wa kuwakusanya. 19 Hakuna uponyaji unaowezekana kwa ajili ya vidonda vyako.

Vidonda vyako ni vikubwa. Wanaosikia habari juu yako watapiga makofi kwa furaha juu yako. Ni nani aliyejiepusha kwa uovu wako wa daima?

# Habakuki

1 Ujumbe ambao habakuki nabii alipokea, 2 Yahwe, kwa muda gani nitalilia msaada,
na hutasikia? Nimekulilia wewe katika kitisho, 'vurugu' lakini hutaniokoa. 3 Kwanini
unanifanya nione mabaya na kuangalia matendo mabaya. Uharibifu na vurugu
uko mbele yangu; kuna mapambano, na ushindani unainuka. 4 Walakini sheria
ni dhaifu, na haki haiishi kwa wakati wowote. Sababu uovu umezunguka haki;
walakini haki ya uongo inatoweka. “Yahwe” anamjibu habakuki 5 “Angalia mataifa
na uwajaribu; stajaabishwa na shangazwa! Sababu nina uhakika kuhusu kufanya
kitu katika siku zako kwamba hutaamini itakapotaarifiwa kwenu. 6 Sababu angalia!
nakaribia kuwainua Wakaldayo - taifa katili na lenye kishindo - wanatembea kupitia
upana wa nchi kuteka nyumba zisizo za kwao. 7 Wanahofu na kuogopa; hukumu
yao na uzuri kutoka kwao unaendelea. 8 Farasi wao pia wanambio sana kuliko
chui, wepesi sana kuliko mbwa mwitu wa jioni. Farasi wao huwaseta, na wapanda
farasi wao wanakuja kutoka mbali - wanapaa kama tai anayewahi kula. 9 Wote
wanakuja kwa vurugu; makundi yao yanakwenda kama upepo wa jangwani, na
wanakusanya mateka kama mchanga. 10 Wanawadhihaki wafalme, na viongozi
ni dhihaka kwaajili yao. Huicheka kila ngome, maana hurundika mavumbi na
kuyaondoa. 11 Ndipo upepo utapita; itaendelea kupita - watu wenye hatia, ambao
uwezo wao ni katika mungu.” Habakuki anamuuliza Yahwe swali lingine 12 “Wewe si
wa tangu nyakati za zamani, Yahwe Mungu wangu, uliye Mtakatifu? Sisi hatutakufa.
Yahwe aliwatenga kwaajili ya hukumu, na ninyi, Mwamba, mmeimarisha kwaajili ya
kusahihisha. 13 Macho yenu ni safi kuangaza juu ya uovu, lakini hamuwezi kuangalia
matendo mabaya kwa fadhila; kwa nini mnaangalia kwa upendeleo hivyo juu ambao
wanasaliti? Kwanini kunyamaza wakati uovu unameza sana wenye haki zaidi yao?
14 unawafanya watu kama samaki baharini, kama vitu vitambaavyo bila kiongozi
juu yao. 15 Wao wanawaleta wote kwa ndoano; wanawakokota watu kutoka kwenye
nyavu za samaki na kuwakusanya kwenye wavu wao. Hii ndiyo sababu wanafurahi
na kupiga kelele kwa uchangamfu sana. 16 Walakini wanatoa sadaka kwenye nyavu
zao za kuvulia na kuchoma ubani kwenye nyavu zao, sababu wanyama wanene ni
sehemu yao, na nyama iliyonona ni chakula chao. 17 Kwa sababu hiyo watamaliza
nyavu zao za kuvulia na kuendelea kuchicha mataifa, bila kuhisi huruma”?

## 2

1 Nitasimama kwenye nguzo yangu ya ulinzi na kujiweka mwenyewe juu ya
mnara wa mlinzi, na nitatazama kwa makini kuona yeye atasema nini kwangu
na namna gani nitageuka kutoka kwenye lawama yangu. 2 Yahwe alinijibu na
alisema, “Rekodi maono haya, na uandike dhahiri juu ya kibao ili kwamba anayesoma
anaweza kukimbia. 3 Sababu maono haya bado ni kwa wakati ujao na hatimaye
atazungumza bila kuanguka. Ingawa inachelewa, isubiri. Sababu kwa hakika
itatakuja na haitachelewa. 4 Tazama! yule ambae hamu yake siyo sawa ndani yake
anapumua kwa nguvu. Lakini mwenye haki ataishi kwa imani. 5 Sababu mvinyo
ni msaliti wa kijana mwenye kiburi ili kwamba asistahimili, lakini hukuza tamaa
yake kama kaburi na, kama kifo, haitaweza kuridhishwa. Yeye anajikusanyia kila
taifa na anakusanya kwaajili yake watu wote. 6 Haya yote hayatatengeneza usemi
kumdhihaki na wimbo wa dhihaka unaomhusu, 'ole wake yule aongezaye visivyo
vya kwake! kwa muda gani utaongeza uzito wa dhamana uliyochukua?' 7 Wale
wanao ngojea kwako hawatainuka ghafla? na wale wanaokutetemesha kuamka?

Utakuwa mwathirika kwaajili yao. [8] Kwasababu umeteka nyara watu wengi, mabaki
yote ya watu, yatakuteka nyara wewe. Sababu umemwaga damu nyingi za watu na
umetenda kwa uasi kinyume cha nchi, miji, na wote wanaokaa ndani yake. [9] Ole
kwa yule anayechonga mapato maovu kwaajili ya nyumba yake, hivyo anaweza
kutengeneza kiota chake juu kumweka yeye salama mbali na mikono ya uovu.
[10] Umebuni aibu kwa nyumba yako kwa kuwakata watu wengi, na umefanya dhambi
dhidi yako mwenyewe. [11] Sababu jiwe litapaza sauti kutoka ukutani, na pao la mbao
litawajibu, [12] 'Ole wake yule ajengaye mji kwa damu, na anayeimarisha mji kwa
katika uovu. [13] Hii haitoki kwa Yahwe wa majeshi kwamba watu wafanye kazi kwa
moto na mataifa yote mengine yanachakaa menyewe bila kitu? [14] Bado nchi itajaa
maarifa ya utukufu wa Yahwe kama maji yanavyojaza bahari. [15] 'Ole wake yule
anayemfanya jirani yake alewe, wewe ambaye unaye ongeza sumu uwafanye walewe
ili uweze kutazama uchi wao. [16] Utavimbiwa na aibu zaidi kuliko utukufu. Kunywa
hiyo vilevile, na funua uchi wako mwenyewe. Kikombe cha mkono wa kuume wa
Yahwe utakuja katika kukugeukia wewe, na aibu itafunika heshima yako. [17] Vurugu
iliyofanywa kwa Lebanoni itakufunika na uharibifu wa wanyama utakuogopesha.
Sababu umemwaga damu za watu na umetenda kwa uasi dhidi ya ile nchi, miji,
na wote wanaokaa humo. [18] Sanamu iliyochongwa inakufaidia nini? Sababu yule
aliyeichonga hiyo, au ambaye kaisubu kwa kuiyeyusha metali, ni mwalimu wa uongo;
Sababu anaiamini kazi ya mikono yake anapotengeneza miungu hii isiyoongea. [19] 'Ole
kwa yule anayeuambia ubao, Amka! Au kwa jiwe lisiloongea, Inuka!' Vitu hivi
vinafundisha? Angalia, hiki juu kimefunikwa kwa dhahabu na fedha, lakini ndani
yake hakipumui kabisa. [20] Lakini Yahwe yumo katika hekalu lake takatifu! Nchi yote
iwe kimya mbele zake.

# 3

[1] Maombi ya Habakuki nabii: [2] Yahwe, nimesikia taarifa zako, na mimi naogopa.
Yahwe, fufua kazi yako katikati wakati; katikati ya muda huu; fanya hiyo ijulikane;
kumbuka kuwa na rehema katika ghadhabu yako. [3] Mungu alikuja kutoka Temani,
na yule Mtakatifu kutoka Parani. Sela. Utukufu wake umezifunika mbingu, na dunia
ilikuwa imejaa utukufu wake. [4] Miali miwili ya mikono yake ilikuwa iking'aa kama
mwanga, ambapo uweza wake ulifichwa. [5] Ugonjwa wa kuua ulitangulia mbele
yake, na adha iliifuta miguu yake. [6] Yeye alisimama na akaipima nchi; aliangalia na
aliyatikisa mataifa. Hata milima ya milele iliharibiwa kabisa, na vilima vya milele
vilianguka chini. Njia yake ni ya milele. [7] Niliona mahema ya Wakushi katika mateso,
na vitambaa vya mahema katika Midiani vinatetema. [8] Yahwe alikuwa na hasira
pale mtoni? Ghadhabu yako ilikuwa dhidi ya mito, au hasira yako dhidi ya bahari,
unapopanda juu ya farasi wenye mikokoteni na wa ushindi wako? [9] Umeleta upinde
wako bila mfuniko; unaweka mishale kwenye upinde wako! Sela. uliigawa nchi
na mito. [10] Milima ilikuona wewe na kugeuka kwa huzuni. Maji yaliyomwagwa
chini yalipita juu yao; kina cha bahari kilipaza sauti. Mawimbi yake yakainuka
juu. [11] Jua na mwezi vilisimama imara juu mahali pake katika mwanga wa mishale
yako na ilipaa, pale katika uangavu wa mwanga wa mikuki yako. [12] Umetembea
juu ya nchi kwa uchungu. Katika ghadhabu umepukuchua mataifa. [13] Ulikwenda
nje kwaajili ya wokovu wa watu wako, Kwaajili ya wokovu wa mteule wako. Wewe
pondaponda kichwa cha nyumba ya mwovu kuweka wazi msingi wa shingo. Sela.
[14] Umekichoma kichwa cha wapiganaji wake kwa mshale wake mwenyewe sababu
walikuja kama upepo kututawanya sisi, wivu wao ulikuwa kama mtu ambaye
anamteketeza masikini katika mahali pamaficho. [15] Umesafiri juu ya bahari kwa
farasi wako, na kuyapita maji makuu. [16] Nilisikia, na ndani yangu nilitetemeka!

midomo yangu ilitetemesha sauti. Uozo unakuja katika mifupa yangu, na chini
yangu mwenyewe nilitetemeka kama nasubiri kwaajili ya siku ya kuhuzunisha ifike
juu ya watu waliotushambulia sisi. 17 Ingawa mtini hauchipui na hauzai kutokana
na mzababibu; na ingawa kuzaa kwa mti wa mzaituni hakuridhishi na mashamba
hayatoi chakula; na ingawa kundi mifugo limetoweka na hakuna ng'ombe katika
zizi, hiki ndicho nitakacho kifanya. 18 Bado, nitafurahia katika Yahwe. Nitakuwa
nafuraha kwa sababu ya Mungu wa wokovu wangu. 19 Bwana Yahwe ni nguvu yangu
na anaifanya miguu yangu kama ya kulungu. Ananifanya mimi niende mbele mahali
pangu pa juu. - kufuata maelekezo ya muziki, katika vyombo vyangu vya nyuzi.

# Sefania

1 Hili ni neno la Yahwe ambalo lilikuja kwa Sefania mwana wa Kushi mwana
wa Gedalia mwana wa Amaria mwana Hezekia, katika siku za Yosia mwana wa
Amoni, mfalme wa Yuda. " 2 Nitaangamiza kabisa kila kitu kutoka usoni mwa
dunia - hili ni tamko la Bwana mwenyewe. 3 Nitamwangamiza mtu na mnyama;
Nitawaangamiza ndege wa mbinguni na samaki wa baharini, uharibifu pamoja
na waovu. Hivyo nitamfutilia mbali mtu kutoka uso wa dunia - hili ni tamko la
Bwana mwenyewe. 4 Nitafika kwa mkono wangu juu ya Yuda na wote wenyeji wa
Yerusalemu. Nitafutilia mbali kila mabaki ya Baali kutoka sehemu hii na majina ya
watu waabuduo sanamu miongoni mwa makuhani, 5 watu ambao juu ya nyumba
huabudu miili ya mbinguni, na watu ambao huabudu na kuapa kwa Yahwe bali
ambao pia huapa kwa mfalme wao. 6 Nitawafutilia mbali pia wale ambao wamegeuka
nyuma kutoka kumfuata Yahwe, wale ambao pia humtafuta Yahwe pasipo kuuliza
ulinzi wake. 7 Uwe kimya mbele ya Bwana Yahwe! Kwa kuwa siku ya Yahwe ni
karibu, Yahwe ameandaa dhabihu na amewatenga wageni wake. 8 "Itakuja katika
siku ya dhabihu ya Bwana, hivyo nitawapiga wakuu na wana wa mfalme, na kila
mmoja aliyevikwa mavazi ya kigeni. 9 Katika siku hiyo nitawapiga wote wale ambao
huruka juu ya kizingiti, wale ambao hujaza nyumba ya bwana wao kwa vurugu na
udanganyifu. 10 Itakuwa katika siku ile - hili ni tangazo la Yahwe - kwamba kilio cha
huzuni kitakuja kutoka kwenye mlango wa samaki, ikipiga yowe kutoka Wilaya ya
Pili, na sauti ya kishindo kikuu kutoka vilimani. 11 Pigeni yowe, wenyeji wa Soko
la Wilaya, kwa wote wafanyabiashara watakuwa wameharibiwa, wote wale ambao
hupima fedha watakuwa wamefutiliwa mbali. 12 Itakuwa katika siku ile nitaitafuta
Yerusalemu kwa taa na kuwapiga wanaume ambao watakuwa wamekaa kwenye
mvinyo wao na kusema mioyoni mwao, 'Yahwe hatafanya chochote, ama kizuri au
kiovu.'. 13 Mali zao zitakuja kuporwa, na nyumba zao zitakuwa zimetelekezwa kwa
maangamizi!. Watajenga nyumba lakini hawataishi humo, na kupanda mizabibu
lakini hawatakunywa mvinyo wake. 14 Siku kubwa ya Yahwe ni karibu, karibu
na inaharakisha upesi! Sauti ya siku ya Yahwe itakuwa ya kilio cha uchungu wa
kishujaa! 15 Siku hiyo itakuwa siku ya ghadabu, siku ya huzuni na uchungu, siku
ya dhoruba na maangamizi, siku ya giza na utusitusi, siku ya mawingu na giza
nene. 16 Itakuwa siku ya parapanda na kengele dhidi ya ngome mijini na buruji
ndefu. 17 Hivyo nitaleta dhiki juu ya wanadamu, kwa hiyo watatembea karibu kama
wanaume vipofu tangu walipofanya dhambi dhidi ya Yahwe. Damu yao itamwagwa
kama vumbi, na sehemu zao za ndani kama kinyesi. 18 Wala fedha zao wala dhahabu
zao hazitaweza kuwaokoa juu ya ghadhabu ya Yahwe. Ndani ya moto wa wivu
wake dunia yote itateketezwa, hivyo ataleta ukamilifu, miwisho wa kutisha kwa wote
wakaao duniani."

## 2

1 Kusanyikeni pamoja ninyi wenyewe mkutano wa hadhara na kusanyikeni,
taifa lisilokuwa na aibu - 2 kabla amri kuchukua madhara na siku hiyo kupita
kama makapi, kabla hasira kali ya ghadhabu ya Yahwe kuja juu yenu, kabla
siku ya ghadhabu ya Bwana kuja juu yenu. 3 Mtafuteni Yahwe, ninyi watu
wote wanyenyekevu duniani mnaozitii amri zake! Tafuteni haki yake. Tafuteni
unyenyekevu, na labda mtalindwa katika siku ya ghadhabu ya Yahwe. 4 hivyo
Gaza utatelekezwa, na Ashkeloni utageuka kuwa uharibifu. Watauondoshea mbali

Ashdodi wakati wa mchana, na wataung'oa Ekroni!. 5 Ole kwa wanaokaa kando ya
bahari, taifa la Wakerethi! Yahwe amesema dhidi yenu, Kanaani, nchi ya Wafilisiti.
Nitawaangamiza hakuna mkazi atakayebakia. 6 Hiyo nchi ya kando ya bahari
itakuwa malisho kwa wachungaji na kwa mazizi ya kondoo. 7 Nchi ya kando ya
bahari itakuwa mali ya mabaki ya watu wa nyumba ya Yuda, watakaochungia
makundi yao huko. Watu wao watalala jioni katika nyumba ya Ashikeloni, kwa
kuwa Yahwe Mungu wao atawatunza na kurejesha wafungwa wao. 8 Nilizisikia
dhihaka za Moabu na wakiwatukana watu wa Amoni wakati walipowadhihaki watu
wangu na kujitukuza mipakani mwao. 9 Kwa hiyo, kama ninavyoishi - hili ni tamko
la Yahwe wa majeshi, Mungu wa Israeli, - Moabu itakuja kuwa kama Sodoma, na
watu wa Amoni kama Gomora; mahali pa viwavi na shimo la chumvi, jangwa la
daima. Lakini watu wangu waliosalia watawateka mateka, na watu wa taifa langu
waliobaki watachukua umiliki wao.' 10 Hili litatokea kwa Moabu na Amoni kwa
sababu ya kiburi chao, tangu walipowadhihaki na kuwatukana watu wa Yahwe
wa majeshi. 11 Ndipo watamwogopa Yahwe, kwa kuwa ataidhihaki miungu yote
ya dunia. Kila mmoja atamwabudu yeye, kila mmoja kutoka mahali pake, kutoka
kila upande wa pwani. 12 Ninyi Wakushi pia mtakufa kwa upanga wangu, 13 na
mkono wa Mungu utaishambulia kaskazini na kuiangamiza Ashuru, Kwa hiyo Ninawi
utatelekezwa kwa kuteketezwa, kuwa pakavu kama jangwa. 14 Ndipo makundi ya
wanyama yatalala pale, kila mnyama wa mataifa, wote kirukanjia na nungunungu
watapumzika juu ya safu zao. Sauti itasikika kutoka madirishani; kifusi kitakuwa
milangoni; nakshi za mwerezi wao mihimili itakuwa imeifunua. 15 huu ni mji wa
kushangiliwa ambao umekaa pasipo hofu, ambaye husema moyoni mwake, “Mimi
niko, na hakuna mwingine wa kufanana na Mimi”. Kwa namna ulivyokuwa wa
kutisha, mahali pa kulala wanyama ndani yake. Kila mmoja ambaye hupitia kwake
huuhisia na kutingisha ngumi kwake.

# 3

1 Ole kwa mji ulioasi! Mji wenye vurugu umenajisiwa. 2 Haukuisikiliza sauti
ya Mungu, wala haukupokea masahihisho kutoka kwa Yahwe. Hakumtumaini
Yahwe na hatamkaribia Mungu wake. 3 Wafalme wao ni simba wanaounguruma
miongoni mwao. Waamuzi wao ni mbwa mwitu wa jioni wasiobakiza kitu ambacho
kitakuwa kimemung'unywa asubuhi yake. 4 Manabii wake wanakiburi na wanaume
wasaliti. Makuhani wake wamepanajisi mahali patakatifu na wameifanyia vurugu
sheria. 5 Yahwe ni mwenye haki miongoni mwao. Hawezi kufanya makosa. Kila
asubuhi husimamia haki yake! Haitafichika nuruni, hata hivyo watu wasio wenye
haki hawajui kuona aibu. 6 Nimeyaharibu mataifa; ngome zao zimeharibiwa.
Nimeifanya mitaa yao magofu, hivyo hakuna hata mmoja anayepitia kwake. Miji
yao imeharibiwa kwa hiyo hakuna mtu anayeikaa. 7 Nikasema, 'Hakika mtaniogopa
mimi. Pokeeni masahihisho na msikatiliwe mbali kutoka kwenye miji yenu kwa
yote yale niliyokuwa nimeyapanga kuyafanya kwenu.' Lakini walikuwa na shauku
kuanza kila siku kwa kuharibu matendo yao yote. 8 Kwa hiyo ningojeni - hili ni tamko
la Yahwe - mpaka siku ambayo nitainuka kwa ajili ya waathirika. Uaamuzi wangu
nikuwakusanya mataifa, kuzikusanya falme, na kumwaga juu yao hasira yangu,
uchungu wangu wote mkali, hivyo nchi yote itamezwa kwa moto wa hasira yangu.
9 Ndipo nitawapa midomo safi watu, kuwaita wote kwa jina la Bwana kunitumikia
wakisimama bega kwa bega. 10 Kutoka ng'ambo ya mto Ethiopia waniabuduo -
watu wangu waliotawanyika - wataleta dhabihu kwa sababu yangu. 11 Katika siku
hiyo hamtawekwa kwenye woga kwa matendo yenu yote ambayo mmeyafanya dhidi
yangu, tangu wakati ule nitaondoa kutoka kwenu wale waliosherehekea fahari yenu,

na kwa sababu hamtakuwa na muda mrefu kufanya majivuno juu ya mlima wangu
mtakatifu. 12 Lakini nitawaacha kama wa chini zaidi na watu masikini, na mtapata
kimbilio katika jina la Yahwe. 13 Mkazi wa Israeli si muda mrefu hatafanya udhalimu
au kusema uongo, na hakuna ulimi wa udanganyifu utakaoonekana mdomoni mwao;
hivyo watalisha na kulala chini, na hakuna hata mmoja atakayewafanya kuogopa."
14 Imba, binti Sayuni! Piga kelele, Israeli. Ufurahi na kushangilia kwa moyo wako
wote, binti wa Yerusalemu. 15 Yahwe ameiondoa hukumu yako; amewafukuzia mbali
adui zako! Yahwe ni mfalme wa Israeli miongoni mwenu. Kamwe hamtamwogopa
tena mwovu!. 16 Katika siku hizo watasema kwa Yerusalemi, "Usiogope, Sayuni.
Usiiache mikono yako ilegee. 17 Yahwe Mungu wako yuko katikati yenu, mwenye
nguvu wa kuwaokoa. Atasherehekea juu yenu na kwa furaha atakuwa kimya juu
yenu kwa upendo wake. Atakuwa na furaha juu yenu na atashangilia kwa furaha,
18 katika siku maalumu ya sherehe. Nitaondoa maafa kutoka kwenu; si muda mrefu
hamtabeba aibu kwa ajili yake. 19 Tazama, Niko tayari kuwashughulikia watesi wenu
wote. Katika wakati ule, Nitawaokoa waliolemaa na kuwakusanya waliotupiliwa
mbali. Nitawafanya kuwa sifa, na nitaibadilisha aibu yao iwe sifa katika dunia
yote. 20 Katika wakati ule nitawaongoza; katika wakati ule nitawakusanya pamoja.
Nitawafanya mataifa yote ya dunia kuwaheshimu na kuwasifu, wakati mtakapoona
hivyo, Nitakuwa nimewarudisha", asema Yahwe.

# Hagai

[1] Katika mwaka wa pili wa mfalme Dario, katika mwezi wa sita, siku ya kwanza
ya mwezi, neno la Bwana likaja kwa kwa mkono wa nabii Haghai kwenda kwa
gavana wa Yuda, Zerubabeli mwana wa Sheatieli na kuhani mkuu Joshua mwana
wa Yehozadaki, kusema, [2] "Bwana wa Majeshi asema: 'Hawa watu husema, "Si
wakati wetu kuja au kujenga nyumba ya Jehova."'" [3] Tena neno la Bwana lilikuja
kwa mkono wa nabii Haghai kusema, [4] "Je ni wakati kwenu wenyewe kuishi katika
nyumba zilizokamilika, na wakati nyumba hii inaharibika? [5] Kwa hiyo sasa Bwana
wa Majeshi asema hivi: 'zitafakarini njia zenu! [6] Mmepanda mbengu nyingi, lakini
mkaleta mavuno kidogo; mnakula lakini hamshibi, mnakunywa lakini hamkujazwa
na vinywaji. Mnavaa nguo lakini hampati joto wenyewe, na mtu wa mshahara hupata
pesa na kuweka kwenye mfuko wenye mashimo tu!' [7] Bwana wa Majeshi asema haya:
[8] 'Zitafakarini njia zetu! Pandeni milimani, mkalete mbao, na mjenge nyumba yangu;
na pia nitakuwa radhi na nitatukuzwa!' Asema Bwana. [9] 'Mmetazamia kupata vingi,
lakini tazama! ulileta nyumbani vichache, nitavitowesha mbali! kwa nini?'- Hivi
ndivyo anatamka Bwana wa Majeshi! kwa sababu nyumba yangu inakaa kwenye
uharibifu, lakini kila mtu yuko radhi kwenye nyumba yake. [10] Kwa sababu hii
mbingu zimeshikiwa zisitoe umande kutoka kwako, na ardhi imeshikilia haizalishi.
[11] Nimekuita kutoka juu ya ardhi na juu ya milima, juu ya nafaka na juu ya mzabibu
mpya, juu ya mafuta na juu ya mavuno ya ardhi, juu ya watu na juu ya wanyama,
na juu ya kazi zote za mikono yako. [12] Kisha Zerubabeli mwana wa Shelitieli, na
kuhani mkuu Yoshua mwana wa Yehozadaki, pamoja na mabaki ya watu, wakati
sauti ya Bwana Mungu wao, na maneno ya Nabii Hagai, kwa sababu Bwana Mungu
wao alikuwa amemtuma. Na watu wakaogopa uso wa Bwana. [13] Ndipo Hagai,
mjumbe wa Bwana, akaongea ujumbe wa Bwana kwa watu na kusema,"'Niko pamoja
na wewe!'- Hili ni tamko la Bwana. [14] Bwana alitibua roho ya mkuu wa mkoa wa
Yudah, Zerubabeli mwana wa Sheltieli, na roho ya kuhani mkuu Joshua mwana wa
Yehozadaki, na roho ya masalia ya watu, kwa kiasi kwamba wakaenda kufanya kazi
katika nyumba ya Bwana Mungu wa majeshi, Mungu wao. [15] katika siku ya ishirini
na Mwezi wa sita, katika mwaka wa pili wa utawala wa Mfalme Dario.

## 2

[1] Katika Mwezi wa saba siku ya ishirini na moja ya mwezi, Neno la Bwana lilikuja
kwa mkono wa Nabii Hagai, na kusema, [2] "Ongea na mkuu wa mkoa wa Yudah,
Zerubabeli mwana wa Sheltieli, na kwa kuhani mkuu Yehozadaki; na kwa masalia
ya watu. Waambie, [3] Ni nani amebaki kati yenu aliuona utukufu wa nyumba ya
kwanza? Na mnauonaje huu wa sasa? Je si kama si chochote machoni penu? [4] Sasa,
muwe hodari, Zerubabeli' -hili ni tamko la Bwana - na uwe hodari, kuhani mkuu
Joshua mwana wa Yehozadaki; muwe hodari, enyi watu wa nchi! - hili ni tamko la
Bwana - na kazi, kwa kuwa ni pamoja nawe! hili ni tamko la Bwana wa majeshi.
[5] Kutegemeana na ahadi ilioko katika agano nililofanya na ninyi mlipotoka Misri
na Roho yangu ilisimama katikati yenu, msiogope' [6] Kwa kuwa Bwana wa majeshi
anasema hivi: 'kitambo kidogo kwa mara nyingine nitatikisa mbingu na dunia, bahari
na nchi kavu! [7] Na nitatikisa kila taifa, na kila taifa wataleta vitu vya thamani
kwangu, na kuijaza nyumba hii na utukufu!' asema Bwana wa Majeshi [8] Dhahabu
na fedha ni yangu' - hili ni tamko la Bwana wa majeshi. [9] Utukufu wa nyumba hii
utakuwa mkuu zaidi ya utukufu wa nyumba ya kwanza ', asema Bwana wa majeshi,'

na nitawapa amani katika sehemu hii'- hili ni Tamko la Bwana wa majeshi 10 Katika
siku ya ishirini na nne mwezi wa tisa, mwaka wa pili wa utawala wa Dario, neno la
Bwana lilimjia nabii Hagaina kusema, 11 “Bwana wa majeshi asema hivi: Muulize
kuhani kuhusu sheria, na kusema: 12 kama mtu akibeba nyama iliyotolewa kwa
Bwana katika pindo la vazi lake, kama upindo utagusa mkate au mchuzi, mvinyo au
mafuta, au chakula kingine, je chakula hicho kinafanyika kitakatifu?”Kuhani alijibu
akasema, “hapana” 13 Halafu Hagai akasema.”Kama mtu mchafu najisi kwa ajili ya
kumgusa maiti na kugusa vitu hivi, wote wanaweza kuwa wachafu?” Kuhani akajibu
na kusema, “Ndiyo, watakuwa wachafu.” 14 Kwa hiyo Haghai akajibu nakusema, “Ni
pamoja na hawa watu na pamoja na taifa liliko mbele yangu! - haya anayasema
Bwana- na pia kila kitu kimekwisha kwa mkono wake: walichotoa hakikuwa kisafi
kilikuwa kichafu. 15 Kwa hiyo, fikiri kutoka siku hii ya leo na za nyuma, kabla hata
jiwe halijawekwa kwenye jiwe lingine katika hekalu la Bwana, 16 ilikuwaje basi? kila
mtu alipokuja kwenye vipimo ishirini vya nafaka, kumbe kulikuwa na vipimo kumi
tu, na aliyekuja na aliyekuja kuchota divai ya vipimo hamsini, kumbe kuliwa na
vipimo ishirini tu. 17 Niliwataabisha ninyi na kazi za mikono yenu kwa doa na koga,
nalikini hamkunirudia'- asema Bwana. 18 tafakari siku hii ya leo na kuendelea, kutoka
siku ya ishirini na nne katika mwezi mwezi wa tisa, toka siku ile msingi wa hekalu
la Bwana kuwekwa. Tafakarini hilo! 19 Je, bado kuna mbegu katika ghala? Mzabibu,
mti wa mtini, komamanga, na mti wa mzeituni havikuzaa matunda! lakini kutoka
siku hii ya leo nitawabariki!”' 20 Tena neno la Bwana likaja kwa mara ya pili kwa
Haghai siku ya ishiri na nne katika mwezi kusema, 21 “Sema na mkuu wa mkoa wa
Yuda, Zerubabeli umwambie, 'Nitatikisa mbingu na dunia. 22 kwa hiyo nitaanhusha
kiti cha falme na kuharibu nguvu ya falme za mataifa! nitaangusha magahari na
wapandao; farasi na wapanda farasi wataanguka, kila mmoja kwa sababu ya upanga
wa ndugu zake. 23 Siku hiyo '-hivi ndivyo asema Bwana wa Majeshi- 'Nitakuchukua
wewe Zerubabeli mwana wa Sheltieli, kama mtumishi wangu'- hivi ndivyo Bwana
anavyosema. “Nitakutuma kama pete ya muhuri wangu, kwa sababu mimi ndiye
niliyekuchagua!'- asema Bwana wa majeshi!”

# Zekaria

[1] Katika mwezi wa nane mwaka wa pili wa kutawala kwake Dario, neno la
Yahwe lilimjia nabii Zekaria, mwana wa Berekia mwana wa Ido, kusema, [2] “Yawhe
alikuwa na hasira sana juu ya baba zenu! [3] Wambie, 'Yahwe wa majeshi asema
hivi: Nirudieni! - nami nitawarudia ninyi, asema Yahwe wa majeshi. [4] Msiwe kama
baba zenu ambao hapo zamani manabii waliwambia, wakisema, “Yahwe wa majeshi
asema hivi: Geukeni kutoka katika njia zenu za mbaya na matendo yenu mabaya!”
Lakini hawakuweza kusikia wala kunijari - asema Yahwe.' [5] Wako wapi baba zenu?
Na manabii, je wapo hapa daima? [6] Lakini maneno yangu na maagizo niliyowaamru
watumishi wangu manabii, je hayakuwapata baba zenu? Hivyo walitubu na kusema,
'Kama vile Yahwe wa majeshi alivyokusudia kututenda kwa kadili zinavyostahili njia
na matendo yetu, ndivyo alivyotutenda.” [7] Katika siku ya ishirini na nne ya mwezi
wa kumi na moja, ndiyo mwezi wa Shebati, mwaka wa pili wa utawala wa Dario,
neno la Yahwe lilimjia nabii Zekaria mwana wa Berekia mwana wa Ido, akasema,
[8] “niliona wakati wa usiku, na tazama! mtu alikuwa amepanda farasi mwekundu,
naye alikuwa kati ya miti ya mihadasi iliyoko bondeni; na nyuma yake kulikuwa
na farasi mwekundu, farasi wa kijivu, na farasi mweupe.” [9] Nikauliza, “ Bwana,
hivi ni vitu gani?” Malaika aliyesema nami akaniambia, “Nitakueleza vitu hivi
ni nini.” [10] Kisha mtu aliyesimama kati ya miti ya mihadasi akajibu na kusema,
“Hawa ndiyo Yahwe aliowatuma kuzunguka katika dunia yote.” [11] Wakamjibu
malaika wa Yahwe aliyekuwa amesimama kati ya miti ya mihadasi na kumwambia,
“Tumekuwa tukizunguka duniani pote; tazama, dunia yote imekaa na kutulia.”
[12] Ndipo malaika wa Yahwe alipojibu na kusema, “Yahwe wa majeshi, hata lini
usiuhurumie Yerusalemu na miji ya Yuda ambayo imeteswa na kudhurumiwa miaka
hii sabini?” [13] Yahwe akamjibu malaika aliyekuwa amesema nami, kwa maneno
mazuri, maneno ya faraja. [14] Hivyo malaika aliyekuwa anaongea nami akaniambia,
“Ita kwa sauti na useme 'Yahwe wa majeshi asema: Nina wivu kwa ajili ya
Yerusalemu yaani Sayuni kwa uchungu mkubwa! [15] Nami nina hasira juu ya mataifa
yaliyo na utulivu. Kwa maana nilikasirika kidogo tu, lakini wao wakasababisha
madhara mabaya. [16] Kwa hiyo Yahwe wa majeshi asema hivi: Nimeirudia Yerusalema
kwa huruma. Hivyo nyumba yangu itajengwa ndani yake - asema Yahwe wa majeshi.
Kipimo kitanyoshwa juu ya Yerusalemu! [17] Ita tena, ukisema, 'Yahwe wa majeshi
asema hivi: Miji yangu kwa mara nyingine itajawa na uzuri, na Yahwe ataifariji
tena Sayuni, na kuichagua Yerusalemu kwa mara nyingine tena.” [18] Kisha nikainua
macho na kuona pembe nne! [19] Nikaongea na malaika aliyesema nami, “Hivi ni vitu
gani? Akanijibu “hizi ni pembe zilisosababisha kutawanyika kwa Yuda, Israeli, na
Yerusalemu.” [20] Kisha Yahwe akanionesha mafundi stadi wanne. [21] Nikasema, “Watu
hawa wanakuja kufanya nini?” Akajibu na kusema, “Hizi ni pembe zililoitawanya
Yuda na hakuna mtu angeweza kuinua kichwa chake. Lakini watu hawa wanakuja
kuziondoa, kutupa chini pembe za mataifa yaliyoinua nguvu zao kinyume cha nchi
ya Yuda na kuisambaza.”

## 2

[1] Kisha nikainua macho yangu na kuona mtu akiwa na timazi mkononi
mwake. [2] Nikamwuliza, “Unakwenda wapi?” Akaniambia, “Ninakwenda kuupima
Yerusalemu ili kujua upana na urefu wake.” [3] Ndipo malaika aliyekuwa anaongea
nami akaondoka na malaika mwingine akaenda kukutana naye. [4] Malaika wa pili

akamwambia, “Nenda uongee na yule kijana umwambie, 'Yerusalemu utakuwa bila
kuta kwa sababu ya wingi wa watu na wanyama ndani yake. [5] Kwa maana Yahwe
asema, Nitakuwa ulinzi wake, na nitakuwa utukufu katikati yake. [6] Kimbieni!
kimbieni! kimbieni kutoka nchi ya kaskazini - asema Yahwe - kwa maana
nimewatawanya kama pepo nne za anga! - Asema Yahwe. [7] Kimbilieni Sayuni
haraka! ninyi mnaokaa na binti Babeli!” Asema Yahwe. [8] Kwa maana baada
ya Yahwe wa majeshi kuniheshimu aliniweka kinyume na mataifa yaliyowateka -
kwani awagusaye, agusa mboni ya jicho la Mungu! - baada ya Yahwe kutenda hivi,
alisema, [9] “Mimi mwenyewe nitatikisa mkono wangu juu yao, nao watakuwa mateka
kwa watumwa wao.” Ndipo mtakapojua kwamba Yahwe wa majeshi amenituma.
[10] “Imba kwa furaha, binti Sayuni, kwa maana mimi mwenyewe nitakaa nawe! -
asema Yahwe [11] Mataifa makubwa yataungana na Yahwe siku hiyo. “Nanyi mtakuwa
watu wangu; kwa kuwa nitakaa kati yenu,” nanyi mtajua kuwa Yahwe wa majeshi
amenituma kwenu. [12] Kwa maana Yahwe ataimilki Yuda kama milki yake halali
katika nchi takatifu na kwa mara nyingine tena atauchagua Yerusalema kwa ajili
yake mwenyewe. [13] Nyamazeni, mbele za Yahwe, ninyi wote wenye mwili, maana
ameinuka kutoka mahali patakatifu pake!

# 3

[1] Kisha Yahwe akanionesha Yoshua kuhani mkuu amesimama mbele za malaika
wa Yahwe na Shetani amesimama mkono wake wa kushoto kumshitaki kwa ajili ya
dhambi. [2] Malaika wa Yahwe akamwambia Shetani, “Yahwe na akukemee, Yahwe,
aliyeuchagua Yerusalemu, akukemee! Je hiki si kinga kilichotolewa motoni” [3] Yoshua
alikuwa na mavazi machafu aliposimama mbele ya malaika. [4] Malaika akawaambia
waliosimama mbele yake, “Mvulisheni hayo mavazi machafu.” Kisha akamwambia
Yoshua, “Tazama! nimeuondoa uovu wako na nitakuvika mavazi safi.” [5] Haya
wamvike kilemba safi kichwani!” Hivyo wakaweka kilemba safi kichwani pa Yoshua
na wakamvika mavazi safi wakati malaika wa Yahwe amesimama kando. [6] Kisha
malaika wa Yahwe akamwagiza Yoshua na kusema, [7] Yahwe wa majeshi asema hivi:
“Ikiwa utatembea katika njia zangu, na kutunza amri zangu, ndipo utakapoisimamia
nyumba yangu na kulinda nyua zangu, kwa maana nitakuruhusu kwenda na kutoka
kati ya wasimamao mbele zangu. [8] WeweYoshua kuhani mkuu na wenzako wanaoishi
nawe! Sikilizeni. Watu hawa ni ishara, kwa kuwa mimi mwenyewe nitamwinua
mtumishi wangu aitwaye Tawi. [9] Tazameni jiwe nililoliweka mbele ya Yoshua. Kuna
macho saba juu ya jiwe hili moja, nami nitaandika maneno juu yake - asema Yahwe
wa majeshi - nami nitaondoa dhambi katika nchi hii kwa siku moja. [10] Katika siku
hiyo kila mtu atamwalika jirani yake kukaa chini ya mzabibu na mtini wake.” asema
Yahwe wa majeshi.

# 4

[1] Ndipo malaika aliyekuwa akiongea nami akageuka na kuniamsha kama mtu
aamshwavyo usingizini. [2] Akaniuliza, “Unaona nini?” Nikasema, “Ninaona kinara
cha taa kimetengenezwa kwa dhahabu tupu, na bakuli juu yake. Kina taa saba juu
yake na mirija mmoja kwa kila taa. [3] Kando yake kuna mizeituni miwili, mmoja
upande wa kulia na mwingine upande wa kushoto.” [4] Kisha nikamwiliza tena na
malaika aliyeongea nami. “Mambo haya yanamaana gani, bwana wangu?” [5] Naye
akanijibu na kusema, Haujui mambo haya yanamaanisha nini?” Nikasema, “ndiyo
sijui bwana wangu.” [6] Hivyo akaniambia, “Hili ni neno la Yahwe kwa Zerubabeli:
lisemalo siyo kwa uwezo wala kwa nguvu, lakini ni kwa Roho wangu, asema Yahwe
wa majeshi. [7] U nini wewe, mlima mrefu? Mbele ya Zerubabeli utakuwa tambarare,
naye ataondoa jiwe la juu kwa kelele ya 'Neema! Neema kwake!” [8] Neno la Yahwe

likanijia kusema, 9 “Mikono ya Zerubabeli imeweka misingi ya nyumba hii nayo
itaimaliza. Ndipo mtakapojua kuwa Yahwe wa majeshi amenituma kwenu. 10 Ni nani
aliyedharau siku ya mambo madogo? Watu hawa wataona jiwe la kupimia mkononi
mwa Zerubabeli, nao watafurahi. (Taa saba ni macho ya Yahwe yanayozunguka
duniani mwote.)” 11 Ndipo nilipomwuliza malaika, Mizeituni hii miwili isimamayo
upande wa kushoto na kulia wa kinara cha taa ni nini?” 12 Nikauliza kwa mara
nyingine tena, “Haya matawi mawili ya mizeituni kando ya mirija miwili ya dhahabu
iliyo na mafuta ya dhahabu yanatiririka kutoka ndani yake? 13 Naye akaniambia, “
Hauvijui vitu hivi ni nini?” Nami nikasema, “Hapana, bwana wangu.” 14 Akasema,
“Hawa ni wana wa mafuta mabichi ya mizeituni wasimamao mbele ya Bwana wa
dunia yote.”

# 5

1 Kisha nikageuka na kuinua macho yangu, nami nikaona, tazama, gombo lirukalo!
2 Malaika akaniuliza, “Unaona nini?” Nikajibu, “Ninaona gombo lirukalo, urefu wake
dhiraa ishirini na upana wake dhiraa kumi.” 3 Ndipo aliponiambia, “Hii ni laana
iendayo juu ya uso wa nchi yote, kwani tangu sasa kila mwivi ataondolewa kulingana
na lisemavyo upande mmoja, wakati kila aapaye kiapo cha uongo ataondolewa
kulingana na lisemavyo upande mwingine, kwa kadili ya maneno yake. 4 “Nitalituma
- asema Yahwe wa majeshi - hivyo litaingia nyumbani mwa mwivi na nyumbani mwa
aapaye kwa uongo kwa jina langu. Litasalia nyumbani mwake na kuteketeza mbao na
mawe yake.” 5 Ndipo malaika aliyekuwa akisema nami alipoenda nje na kuniambia,
“Inua macho yako uone kinachokuja!” 6 Nikasema, “Ni nini hiki?” Akasema,
“Hiki ni kikapu kilicho na efa ijayo. Huu ni uovu wao katika nchi yote.” 7 Kisha
mfuniko wa risasi ukainuliwa kutoka ndani ya kikapu na kulikuwa na mwanamke
chini yake amekaa ndani yake! 8 Malaika akasema, “Huu ni uovu!” na akamtupa
tena kikapuni, na kurusha mfuniko wa risasi mlango pake. 9 Nilipoinua macho
nikaona wanawake wawili wakija kwangu, na upepo ulikuwa ndani ya mabawa yao
- walikuwa na mabawa kama mabawa ya korongo. Wakainua kikapu kati ya mbingu
na nchi. 10 Hivyo nikamwuliza malaika aliyesema nami, “Wanapeleka wapi kikapu?”
11 Akaniambia, “Wanakwenda kujengea hekalu katika nchi ya Shinari kwa ajili yake,
hekalu litakapokuwa tayari, kikapu kitawekwa kwenye msingi ulioandaliwa kwa ajili
yake.”

# 6

1 Kisha nikageuka na kuinua macho na nikaona vibandawazi vinne vya farasi
vikija kutoka kati ya milima miwili; na milima hiyo ilikuwa imetengenezwa kwa
shaba. 2 Kibandawazi cha kwanza kilikuwa na farasi wekundu, kibandawazi cha
pili kilikuwa na farasi weusi, 3 kibandawazi cha tatu kilikuwa na farasi weupe, na
kibandawazi cha nne kilikuwa na farasi wa kijivu. 4 Hivyo nikamwuliza malaika
aliyesema nami, “Ni vitu gani hivi bwana wangu?” 5 Malaika akajibu na kuniambia,
“Hizi ni pepo nne za mbinguni zisimamazo mbele ya Bwana wa dunia yote. 6 Lenye
farasi weusi linakwenda nchi ya kaskazini; farasi weupe wanakwenda nchi ya
magharibi; na farasi wa kijivu wanakwenda nchi ya kusini.” 7 Farasi hawa wenye
nguvu walitoka na wanatafuta kwenda na kuzunguka juu ya nchi, hivyo malaika
akasema, “Nendeni na mzunguke juu ya nchi!” nao wakaenda juu ya dunia yote.
8 Kisha akaniita na kuniambia, “Tazama wale wanaokwenda nchi ya kaskazini,
wataituliza roho yangu juu nchi hiyo.” 9 Hivyo neno la Yahwe likanijia kusema,
10 “Chukua sadaka kutoka kwa waliohamishwa - kutoka kwa Helidai, Tobiya na
Yedaya - leo hii uende na kuipeleka katika nyumba ya Yosia mwana wa Zefania,

aliyetoka Babeli. 11 Kisha uchukue fedha na dhahabu, ufanye taji na uivike katika
kichwa cha Yoshua mwana wa Yehosadaki kuhani mkuu. 12 Ongea naye na useme,
Yahwe wa majeshi asema hivi: Mtu huyu, jina lake Tawi! Naye atakuwa alipo na kisha
atajenga hekalu la Yahwe! 13 Ndiye atakayejenga hekalu la Yahwe naye atauinua
utukufu wake; kisha ataketi na kutawala katika kiti chake cha enzi. Atakuwa kuhani
juu ya kiti cha enzi na ufahamu wa amani utakuwa kati ya vyote viwili. 14 Taji
itawekwa hekaluni mwa Yahwe kwa heshima ya Heldai, Tobiya na Yedaya na kama
kumbukumbu ya ukarimu wa mwana wa Zefania. 15 Ndipo waliombali watakapokuja
na kulijenga hekalu la Yahwe, hivyo mtajua kuwa Yahwe wa majeshi amenituma
kwenu; kwani ikiwa kweli mnaisikiliza sauti ya Yahwe Mungu wenu hili litatendeka!"

# 7

1 Mwaka wa minne wa utawala mfalme Dario, siku ya nne ya mwezi wa
Kisleu(ambao ni mwezi wa tisa), neno la Yahwe lilimjia Zekaria kusema. 2 Watu
wa Betheli wamemtuma Shareza, Regemu Meleki na watu wao kuomba mbele ya
uso wa Yahwe. 3 Wakaongea na makuhani waliokuwa katika nyumba ya Yahwe
wa majeshi na kwa manabii; wakasema, "Je niomboleze katika mwezi wa tano kwa
njia ya kufunga, kama nilivyofanya miaka mingi hii?" 4 Ndipo neno la Yahwe wa
majeshi liliponijia kusema, 5 "Ongea na watu wote wa nchi na makuhani uwaambie,
"Mlipofunga na kuomboleza katika mwezi wa tano na wa saba katika hii miaka
sabini, je kweli mlifunga kwa ajili yangu? 6 Na mlipokula na kunywa, hamkula
na kunywa kwa ajili yenu wenyewe? 7 Je hayo siyo maneno aliyosema Yahwe kwa
vinywa vya manabii wa zamani, mlipokuwa bado mnaishi Yerusalemu na miji ya
kandokando yenye mafanikio na iliyokaa Negebu, na upande wa magharibi chini ya
vilima?" 8 Neno la Yahwe likamjia Zekaria kusema, 9 "Yahwe wa majeshi asema hivi,
'Hukumuni kwa haki, uaminifu wa agano, na rehema. Kila mtu na amtendee hivi
ndugu yake. 10 Juu ya mjane na yatima, mgeni, na masikini - usiwanyanyase, na
asiwepo miongoni mwenu anayepanga madhara yoyote dhidi ya mwingine mioyoni
mwenu. 11 Lakini waliyashupaza mabega yao na hawakujari. Waliziba masikio yao
ili wasisikie. 12 Waliifanya mioyo yao kuwa migumu kama mwamba ili wasiisikie
sheria au neno la Yahwe wa majeshi. Alipeleka ujumbe kwa watu nyakati za zamani
kwa Roho wake, kwa vinywa vya manabii. Lakini watu hawakusikia, hivyo Yahwe
wa majeshi aliwakasirikia sana. 13 Hata ikawa alipoita hawakusikia. Vilevile," asema
Yahwe wa majeshi, "wataniita, lakini sitasikiliza. 14 Kwa maana nitawatawanya kwa
upepo wa kisurisuri katika mataifa yote ambayo hawajawai kuyaona, na baada yao
nchi itakuwa wazi. Kwa kuwa hakuna hata mmoja atakayepita au kukaa katika hiyo
nchi kwa kuwa wameigeuza nchi yao yenye kupendeza kuwa isiyofaa.

# 8

1 Neno la Yahwe wa majeshi likanijia kusema, 2 "Yahwe wa majeshi asema hivi:
Nina huzuni kwa ajili ya Sayuni kwa wivu mkuu na ninamaumivu kwa hasira nyingi!
3 Yahwe wa majeshi asema hivi: Nitairudia Sayuni nami nitakaa kati ya Yerusalemu,
kwa kuwa Yerusalemu itaitwa mji wa kweli na mlima wa Yahwe wa majeshi utaitwa
Mlima Mtakatifu! 4 Yahwe wa majeshi asema hivi: Kwa mara nyingine tena kutakuwa
na vikongwe katika mitaa ya Yerusalemu, na kila mtu ataitaji mkongojo mkononi
mwake kwa vile alivyo mzee. 5 Pia mitaa ya mji itajazwa na vijana wa kiume na kike
wachezao. 6 Yahwe wa majeshi asema hivi: ikiwa jambo laonekana haliwezekani
katika macho ya masalia ya watu hawa katika siku hizo, je haliwezekani pia machoni
pangu? - asema Yahwe. 7 Yahwe wa majeshi asema hivi: Tazama, nipo tayari
kuwaokoa watu wangu kutoka nchi ya mawio na ya machweo ya jua! 8 Kwa maana

nitawarudisha tena, nao wataishi ndani ya Yerusalemu, hivyo watakuwa watu wangu
tena, nami nitakuwa Mungu wao katika kweli na utakatifu! 9 Yahwe wa majeshi
asema hivi: Ninyi mnaoendelea kusikia maneno yaleyale yaliyotoka katika vinywa
vya manabii msingi wa nyumba yangu ulipowekwa - hii nyumba yangu, Yahwe wa
majeshi: Itieni nguvu mikono yenu ili hekalu lijengwe. 10 Kwani kabla ya siku hizo
hakuna mazao yaliyokusanywa na yeyote ndani yake, hakukuwa na faida siyo kwa
mtu hata mnyama, na hakukuwa na amani kutoka kwa adui kwa kila aliyekwenda au
kuja. Nilimfanya kila mtu kuwa kinyume cha mwenzake. 11 Lakini sasa haitakuwa
kama mwanzo, nitakuwa pamoja na masalia ya watu hawa - asema Yahwe wa
majeshi. 12 Kwani mbegu za amani zitapandwa; mzabibu unaokua utatoa matunda
yake na nchi itatoa mazao yake; anga zitatoa umande, kwa maana nitawapa masalia
ya watu hawa kumilki haya yote. 13 Ulikuwa mfano wa laana kwa mataifa mengine,
enyi nyumba ya Yuda na nyumba ya Israeli. Hivyo nitawaokoa nanyi mtakuwa
baraka. Msiogope; haya mikono yenu itiwe nguvu! 14 Kwa maana Yahwe wa majeshi
asema hivi: Kama nilivyopanga kuwatenda mabaya babu zenu walipochokoza hasira
yangu - asema Yahwe wa majeshi - na wala sikujuta, 15 ndivyo nitakavyoazimia
kuutenda mema tena Yerusalemu na nyumba ya Yuda katika siku hizi! Msiogope!
16 Haya ndiyo mambo mnayopaswa kufanya: Kasemeni kweli, kila mtu na jirani yake.
Hukumuni kwa haki, usawa na amani katika malango yenu. 17 Na asiwepo miongoni
mwenu anayeazimu uovu moyoni mwake dhidi ya jirani yake, wala kuvutwa na
viapo vya uongo; kwani haya yote ndiyo mambo ninayoyachukia! - asema Yahwe."
18 Kisha neno la Yahwe wa majeshi likanijia kusema, 19 "Yahwe wa majeshi asema
hivi: Mifungo ya mwezi wa nne, mwezi wa tano, mwezi wa saba na mwezi wa
kumi itakuwa nyakati za furaha ya kila aina, kwa nyumba ya Yuda! Kwa hiyo
pendeni kweli na amani! 20 Yahwe wa majeshi asema hivi: Watu watakuja tena,
hata wanaoishi miji mingine. 21 Watu wa mji mmoja watakwenda mji mwingine na
kusema, "Haya twendeni haraka mbele ya Yahwe tukaombe na kumtafuta Yahwe
wa majeshi! Sisi wenyewe tunakwenda pia. 22 Watu wengi na mataifa yenye nguvu
yatakuja kumtafuta Yahwe wa majeshi huko Yerusalemu na kuomba upendeleo kwa
Yahwe! 23 Yahwe wa majeshi asema hivi: Katika siku hizo watu kumi kutoka katika
kila lugha na taifa watashika upindo wa kanzu zenu na kusema, "Haya sisi nasi
tutakwenda pamoja nanyi, kwani tumesikia kwamba Mungu yu pamoja nayi!"

# 9

1 Hili ni tamko la neno la Yahwe kuhusu nchi ya Hadraki na Damesiki. Kwa
maana jicho la Yahwe liko juu ya wanadamu wote, na juu ya kabila zote za Israeli
pia. 2 Azimio hili pia linaihusu Hamathi, inayopakana na Damesiki, na linahusu
Tiro na Sidoni, japokuwa ni werevu sana. 3 Tiro amejijengea ngome na kurundika
fedha kama mavumbi na dhahabu safi kama matope mitaani. 4 Tazama! Bwana
atamnyang'anya na kuharibu nguvu zake juu ya bahari, kwa hiyo atateketezwa kwa
moto. 5 Ashikeloni ataona na kuogopa! Gaza pia atatemeka sana! Ekroni, tumanini
lake litatikiswa! Mfalme ataangamizwa kuanzia Gaza, na Ashikeloni haitakuwa na
watu tena! 6 Wageni watafanya makao yao katika Ashidodi, nami nitakiondoa kiburi
cha Wafilisiti. 7 Kwani nitaondoa damu yao katika vinywa vyao na machukizo yao
kutoka kati ya meno yao. Ndipo watakapokuwa masalia kwa Mungu wetu kama
ukoo katika Yuda, na Ekironi atakuwa kama Wayebusi. 8 Nitaweka kambi kuzunguka
nchi yangu kinyume cha majeshi ya adui hata hakuna atakayeweza kupita ndani
yake tena, kwani hakuna mtesaji atakayeipita tena. Kwa kuwa sasa nitaangalia
nchi yangu kwa macho yangu mwenyewe! 9 Piga kelele kwa furaha, ewe binti
Sayuni! Piga kelele kwa shangwe, ewe binti Yerusalem! Tazama! Mfalme wako

anakuja kwako pamoja na uadilifu na anakuokoa. Ni mnyenyekevu, amepanda
punda, mwanapunda. 10 Ndipo nitakapoondoa kibandawazi kutoka Efraimu na farasi
kutoka Yerusalemu, na upinde utaondolewa katika vita; kwani atasema amani kwa
mataifa, na utawala wake utakuwa kutoka bahari hata bahari, na kutoka katika
mto hadi miisho ya dunia! 11 Lakini kwenu, kwa sababu ya damu ya agano langu
nanyi, nitawaweka wafungwa wenu huru kutoka shimoni pasipo na maji. 12 Rudini
ngomeni, wafungwa wa matumaini! Hata leo natamka kwamba nitawarudishia
mara mbili, kwani nimempinda Yuda kama upinde wangu. 13 Hata nimelijaza podo
langu pamoja na Efraimu. Nimewainua wana wenu, Sayuni, kinyume cha wana
wenu, Ugiriki, na amekufanya wewe, Sayuni, kama upanga wa shujaa! 14 Yahwe
atawatokea, na mishale yake itapiga kama radi! Kwa maana Yahwe Bwana wangu
atapiga tarumbeta naye ataendelea pamoja na dhoruba kutoka Temani. 15 Yahwe
wa majeshi atawatetea, nao watawararua na kuyashinda mawe ya kombeo. Ndipo
watakapo kunywa na kupiga kelele kama mtu aliyelewa kwa mvunyo, nao watajazwa
na mvinyo kama mabakuri, kama pembe za madhabahu. 16 Hivyo Yahwe Mungu
wao atawaokoa siku hiyo; watakuwa kama kundi la kondoo lililo na watu wake,
kwani watakuwa mapambo ya taji, yaliyoinuliwa juu ya nchi yake. 17 Jinsi gani
watakavyokuwa wazuri na warembo! vijana watastawi juu ya nafaka na bikra juu
ya divai tamu!

# 10

1 Mwombeni Yahwe mvua nyakati za kipupwe - Yahwe afanyaye mvua ya radi
- naye hufanya mvua inyeshe kwa kila mmoja na uoto kondeni. 2 Kwani sanamu
za wenye nyumba husema uongo; waganga hunena uongo; wanasema ndoto za
udanganyifu na hutoa faraja tupu, hivyo wapotea kama kondoo na wanaumia kwa
sababu hakuna mchungaji. 3 Gadhabu yangu inawaka dhidi ya wachungaji; ni
mabeberu - viongozi - nitakao waadhibu. Yahwe wa majeshi atalihudumia pia
kundi la kondoo wake, nyumba ya Yuda, na kuwafanya kama farasi wake wa
vita! 4 Kutoka kwao litatoka jiwe kuu la pembeni; kutoka kwao kitatoka kigingi
cha hema; kutoka kwao utatoka upinde wa vita; kutoka kwao watakuja viongozi
wote kwa pamoja. 5 Watakuwa kama mashujaa wawakanyagao adui zao katika
matope ya mitaani vitani; watafanya vita, kwa maana Yahwe yu pamoja nao,
nao watawaabisha wapanda farasi wa vita. 6 Nitaitia nguvu nyumba ya Yuda na
kuiokoa nyumba ya Yusufu; kwani nitawarejesha na kuwahurumia. Watakuwa kama
nilikuwa sijawaondoa, kwani mimi ni Yahwe Mungu wao, nami nitawaitikia. 7 Ndipo
Efraimu atakapokuwa kama shujaa, na mioyo yao itafurahi kama kwa mvinyo;
wana wao wataona na kufurahi. Mioyo yao itanifurahia! 8 Nitawanong'oneza
na kuwakusanya, kwani nitawaokoa, nao watakuwa wakuu kama walivyokuwa
mwanzo! 9 Niliwapanda kati ya watu, lakini watanikumbuka katika nchi ya mbali,
hivyo wao na wana wao wataishi na kurejea. 10 Kwa maana nitawarejesha kutoka
nchi ya Misri na kuwakusanya kutoka Ashuru. Nitawaleta katika nchi ya Gileadi
na Lebanoni mpaka kutakapokuwa hakuna nafasi tena kwa ajili yao. 11 Nitapita
katika bahari ya mateso yao; nitayapiga mawimbi ya bahari hiyo na nitavikausha
vilindi vyote vya Nile. Utukufu wa Ashuru utashushwa chini, na fimbo ya Misri
itakwenda mbali kutoka kwa Wamisri. 12 Nitawatia nguvu katika mimi mwenyewe,
nao watatembea katika jina langu - asema Yahwe.

# 11

1 Fungua milango yako, ee Lebanoni, ili moto uteketeze mielezi yako! 2 Omboleza,
enyi miti ya misonobari, kwani mierezi imeanguka! Kilichokuwa cha fahari

kimeteketezwa! Ombolezeni, enyi mialoni ya Bashani, kwani msitu wenye
nguvu umeshushwa. 3 Wachungaji wanapiga yowe, kwa kuwa utukufu wao
umeharibiwa! Sauti ya mungurumo wa wana simba, kwa kuwa kiburi cha Mto
Yordani kimeharibiwa! 4 Hivi ndivyo asemavyo Yahwe Mungu wangu, “Lichungeni
kundi la kondoo lililotiyari kuchinjwa! 5 (Wanaowanunua wanawachinja bila
kuhadhibiwa, nao wawauzao husema, 'Atukuzwe Yahwe! Nimetajirika! Kwa maana
wachungaji wafanyao kazi kwa wenye kondoo hawawahurumii.) 6 Kwa maana hiyo
sitawahurumia tena wenyeji wa nchi! - hivi ndivyo asemavyo Yahwe. Tazama!
Mimi mwenyewe nipo tiyari kumwelekeza kila mtu katika mkono wa jirani yake
na katika mkono wa mfalme wake, nao wataiharibu nchi na hakuna hata mmoja
wao nitakayemwokoa kutoka katika mkono wao.” 7 Hivyo nikawa mchungaji wa
kondoo walioamriwa kuchinjwa, kwa wanaowashughulikia kondoo. Nilichukua
fimbo mbili; fimbo moja nikaiita “Neema” na nyingine nikaiita “Umoja.” Kwa njia hii
niliwachunga kondoo. 8 Ndani ya mwezi mmoja niliwaangamiza wachungaji watatu,
kwa maana sikuwavumilia tena, wao pia walinichukia. 9 Ndipo nilipowaambia
wamiliki, “Sitafanya kazi kama mchungaji wenu tena. Wakondoo wafao - na
wafe; kondoo wanaoangamizwa - na waangamizwe. Na kondoo wasaliao kila
mmoja ale nyama ya jirani yake.” 10 Hivyo nikaichukua fimbo yangu “Neema” na
nikaivunja kuvunja agano nililokuwa nimelifanya na kabila zangu zote. 11 Katika
siku hiyo agano lilivunjwa, na wale wanaoshughulika na kondoo na waliokuwa
wakiniangalia walifahamu kwamba Yahwe amesema. 12 Nikawaambia, “Ikiwa
itawapendeza, nilipeni ujira wangu. Kama sivyo, msifanye hivyo.” Hivyo wakapima
ujira wangu - vipande thelathini vya fedha. 13 Kisha Yahwe akaniambia, “Weka fedha
katika hazina, thamani nzuri zaidi ambayo walikupa!” Hivyo nikachukua vipande
thelathini vya fedha na kuviweka katika hazina ndani ya nyumbani Yahwe. 14 Kisha
nikavunja fimbo yangu ya pili, “Umoja,” kuvunja undugu kati ya Yuda na Israeli.
15 Yahwe akaniambia, “Tena, chukua chombo cha mchungaji mpumbavu kwa ajili
yako mwenyewe, 16 kwa maana tazama, niko tiyari kumweka mahali mchungaji
katika nchi. Hataangalia kondoo wanaoangamia. Hatatafuta kondoo wapoteao, wala
kuwaponya kondoo wachechemeao. Hatawalisha kondoo wenye afya, lakini atakula
nyama ya kondoo walionona naye atapasua kwato zao. 17 Ole kwa wachungaji
wasiofaa wanaoliacha kundi la kondoo! Upanga na uje dhidi ya mkono wake na
jicho lake la kulia! Mkono wake na ukauke na jicho lake la kulia lipofuke!

# 12

1 Hili ni tamko la neno la Yahwe kwa Israeli - Bwana asema, azitandaye mbingu na
kuweka msingi wa dunia, aiumbaye roho ya mtu ndani yake, 2 “Tazama, nitaifanya
Yerusalemu kuwa kikombe kiwafadhaishacho watu wote wamzungukao. Itakuwa
hivyo hivyo pia kwa Yuda wakati wa kuhusuriwa kwa Yerusalemu. 3 Katika siku hiyo,
nitaifanya Yerusalemu kuwa jiwe zito kwa watu wa jamaa zote. Kila atakayejaribu
kuliinua jiwe hilo atajihumiza sana, na mataifa yote ya dunia yatakusanyika kinyume
cha mji huo. 4 Katika siku hiyo asema Yahwe - nitampiga kila farasi kwa ushangao na
kila mpanda farasi kwa wendawazimu. Nitaiangalia nyumba ya Yuda kwa upendeleo
na nami nitawapiga kwa upofu farasi wa majeshi. 5 Ndipo watawala wa Yuda
watakapojisemea mioyoni mwao, 'Wakaao Yerusalemu ndio nguvu yetu kwa sababu
ya Yahwe wa majeshi, Mungu wao.' 6 Katika siku hiyo nitawafanya watawala wa
Yuda kuwa kama mitungi ya moto katika miti na kama miali ya moto kati ya nafaka
isimamayo, kwani utateketeza watu wote walio karibu upande wao wa kulia na
kushoto. Yerusalemu atakaa mahali pake tena. 7 Yahwe ataziokoa hema za Yuda
kwanza, ili kwamba utukufu ya nyumba ya Daudi na utukufu wa wale waishio

Yerusalemu hautazidi sehemu iliyosalia ya Yuda. 8 Katika siku hiyo Yahwe atakuwa
mtetezi wa wakao Yerusalemu, na siku hiyo waliodhaifu miongoni mwao watakuwa
kama Daudi, wakati nyumba ya Daudi watakuwa kama Mungu, kama malaika
wa Yahwe mbele yao. 9 "Itakuwa kwamba katika siku hiyo nitaanza kuyaharibu
mataifa yote yajayo kinyume cha Yerusalemu. 10 Lakini nitamwaga roho ya huruma
na kuiombea nyumba ya Daudi na wakao Yerusalemu, hivyo wataniangalia mimi,
waliomchoma kwa mkuki. Wataniombolezea, kama amwombolezeaye mwana wa
pekee; watamwombolezea kwa uchungu sana kama aombolezaye kifo cha mzaliwa
wa kwanza. 11 Katika siku hiyo maombolezo huko Yerusalemu yatakuwa kama
maombolezo ya Hadadi Rimoni katika tambarare za Megido. 12 Nchi itaomboleza,
kila ukoo peke yao. Ukoo wa nyumba ya Daudi utakuwa peke yake na wake zao
watakuwa peke yao mbali na wanaume. Ukoo wa nyumba ya Nathani utakuwa
peke yao na wake zao watakuwa peke yao mbali na waume. 13 Ukoo wa nyumba
ya Lawi utakuwa peke yao na wake zao watakuwa peke yao mbali na waume. Ukoo
wa Washimei utakuwa peke yao na wake zao watakuwa peke yao mbali na waume.
14 Kila ukoo uliosalia - kila mmoja utakuwa peke yake na wake watakuwa pekee mbali
na waume.

# 13

1 Katika siku hiyo kijito kitafunguliwa kwa ajili ya nyumba ya Daudi na wenyeji
wa Yerusalemu, kwa ajili ya dhambi na uchafu wao. 2 Katika siku hiyo - asema
Yahwe wa majeshi - kwamba nitaondoa majina ya sanamu katika nchi ili kwamba
yasikumbukwe tena. Nitawaondoa pia katika nchi manabii wa uongo na roho
wao mchafu 3 Ikiwa mtu yeyote ataendelea kutoa unabii, baba yake na mama
yake waliomzaa watamwambia, 'Hautaishi, kwa kuwa umenena uongo kwa jina la
Yahwe! Ndipo baba na mama waliomzaa watakapomchoma wakati akitabiri. 4 Katika
siku hiyo kila nabii ataonea aibu maono yake aelekeapo kutoa unabii. Manabii
hawa hawatavaa tena vazi la singa, ili kuwadanganya watu. 5 Kwa maana kila
mmoja atasema, 'Mimi siyo nabii! mimi ni mkulima, kwa maana ardhi ndiyo kazi
yangu tangu ujana wangu! 6 Lakini mtu mwingine atamwambia, 'Majeraha haya
kati ya mikono yako ni ya nini?' naye atajibu, nilijeruhiwa na waliokuwa katika
nyumba ya rafiki zangu." 7 Upanga! inuka mwenyewe dhidi ya mchungaji wangu,
mtu asimamaye karibu nami - hivi ndivyo asemavyo Yahwe wa majeshi. Mpige
mchungaji, na kondoo watatawanyika! Kwa maana nitageuza mkono wangu dhidi
ya wadogo. 8 Kisha itakuwa kwamba katika nchi yote - hivi ndivyo asemavyo Yahwe
- kwamba theluthi mbili yake itaondolewa! Watu hao wataangamia; theluthi moja
tu ndiyo itakayosalia. 9 Nitaipitisha hiyo ya tatu motoni na kuwasafisha kama fedha
isafishwavyo; nitawajaribu kama dhahabu ijaribiwavyo. Wataliitia jina langu nami
nitawajibu na kusema, 'Hawa ni watu wangu!' nao watasema, Yahwe ndiye Mungu
wangu!"

# 14

1 Tazama! Siku ya Yahwe inakuja wakati mateka wenu watakapogawanywa katikati
yenu. 2 Kwa maana nitayakusanya mataifa yote kinyume cha Yerusalemu kwa
vita na mji utatekwa. Nyumba zitatekwa na wanawake watabakwa. Nusu ya mji
itapelekwa matekani, lakini kumbukumbu ya watu haitaondolewa mjini. 3 Lakini
Yahwe ataondoka na kufanya vita dhidi ya mataifa kama apigavyo vita katika siku
ya vita. 4 Siku hiyo miguu yake itasimama juu ya Mlima wa Mizeituni, uliopo kando
ya Yerusalemu upande wa mashariki. Mlima wa Mizeituni utagawanyika katikati kati
ya mashariki na magharibi kwa bonde kubwa sana na nusu ya mlima itarudi nyuma
kuelekea kaskazini na nusu kuelekea kusini. 5 Ndipo mtakapokimbia katika bonde

kati ya milima ya Yahwe, kwa kuwa bonde kati ya hiyo milima litafika hata Azali.
Mtakimbia kama siku mliyokimbia tetemeko la nchi siku za Uzia, mfalme wa Yuda.
Ndipo Yahwe Mungu wangu atakapokuja na watakatifu wake wote. 6 Hakutakuwa
na nuru katika siku hiyo, lakini hakuna baridi wala barafu. 7 Siku hiyo, siku aijuaye
Yahwe peke yake, hakutakuwa tena na mchana wala usiku, kwani jioni itakuwa
wakati wa nuru. 8 Siku hiyo maji yaliyo hai yatatiririka kutoka Yerusalemu. Nusu
yake yatatiririka kuelekea bahari ya mashariki na nusu bahari ya magharibi, wakati
wa masika na wakati wa kiangazi. 9 Yahwe atakuwa mfalme juu ya dunia yote. Katika
siku hiyo kutakuwa na Yahwe, Mungu mmoja, na jina lake pekee. 10 Nchi yote itakuwa
kama Araba, kuanzia Geba hadi Rimoni kusini mwa Yerusalemu. Na Yerusalemu
itaendelea kuwa juu. Ataishi mahali pake mwenyewe, kutoka lango la Benjamini
hata mahali lilipokuwa lango la kwanza, hata Lango la Pembeni, na kutoka Mnara wa
Hananeli hata shinikizo la mfalme. 11 Watu watakaa Yerusalemu na hakutakuwa na
maangamizi kamili tena kutoka kwa Mungu dhidi yao. Yerusalemu itakuwa salama.
12 Hii itakuwa tauni ambayo kwayo Yahwe atawapiga jamaa zote za watu wapigao
vita juu ya Yerusalemu: miili yao itaoza hata wakiwa wamesimama kwa miguu
yao. Macho yao yataoza katika matundu yake na ndimi zao zitaoza katika vinywa
vyao. 13 Siku hiyo ile hofu kuu kutoka kwa Yahwe itakuwa miongoni mwao. Kila
mmoja ataushika mkono wa mwingine, na mkono wa mwingine utainuliwa kinyume
cha mkono wa mwenzake. 14 Yuda pia atapigana na Yerusalemu. Watakusanya
utajiri wa mataifa yote yanayowazunguka - dhahabu, fedha, na wingi wa nguo safi.
15 Tauni itakuwa pia juu ya farasi na nyumbu, ngamia na punda, na kila mnyama
katika kambi hizo atapigwa kwa hilo pigo. 16 Kisha itakuwa wote watakaosalia
katika mataifa yaliyo kinyume na Yerusalemu watakwenda mwaka kwa mwaka
kumwabudu mfalme, Yahwe wa majeshi, na kutunza Sikukuu ya Vibanda. 17 Na
itakuwa kwamba ikiwa mtu yeyote kutoka katika mataifa yote ya dunia haendi
Yerusalemu kumwabudu mfalme, Yahwe wa majeshi, ndipo Yahwe hataleta mvua
juu yao. 18 Na ikiwa nchi ya Misri hawatakwenda, ndipo hawatapata mvua. Tauni
kutoka kwa Yahwe itayashambulia mataifa yote yasiyokwea kutunza Sikukuu ya
Vibanda. 19 Hii itakuwa ni adhabu kwa Misri na adhabu kwa kila taifa lisilopanda
kutunza Sikukuu ya Vibanda. 20 Lakini katika siku hiyo, kengele za farasi zitasema,
“Jitengeni kwa ajili ya Yahwe,” na makalai katika nyumba ya Yahwe yatakuwa kama
mabakuri mbele ya madhabahu. 21 Kwa kuwa kila chungu katika Yerusalemu na
Yuda kitatengwa kwa ajili ya Yahwe wa majeshi na kila mmoja aletaye sadaka atakula
ndani yake na kuyachemshia. Hakutakuwa na wafanyabiashara tena katika nyumba
ya Yahwe wa majeshi siku hiyo.

# Malaki

1 Tamko la neno la Bwana kwa Israeki kwa mkono wa Malaki. 2 “Nilikupenda,
“asema Bwana. Lakini unasema, “kwa jinsi gani ulitupenda?” Esau siyo ndugu
yake Yakobo?” asema Bwana. “Na bado nampenda Yakobo, 3 lakini nimemchukia
Esau. nimeifanya milima yake kuwa ukiwa, na nimepafanya urithi wake kuwa
makao ya mbweha wa jangwani.” 4 Kama Edomu husema, “Tumepigwa, lakini
tutarudi na kujenga palipoharibiwa; “Bwana wa Majeshi asama hivi, “Watajenga
lakini nitaiangusha chini; na wanaume watawaita 'Nchi ya uovu', na 'Watu ambao
ambao Mungu ana hasira nao milele.”' 5 kwa macho yenu mtaona hili, na mtasema,
“Bwana ni mkuu mbele ya mipaka ya Israel.” 6 mtoto amtiibaba yake, na mtumwa
amtii bwana wake. ikiwa mimi, ni baba, iko wapi heshima yangu? na kama mimi ni
bwana, iko wapi heshima yangu? Bwana wa majeshi asema hivi kwenu, makuhani,
mnaodharau jina langu. lakini mnasema, 'tumeridharauje jina lako? 7 kwa kutoa
mikate iliyonajisi madhabahuni kwangu. Na mnasema kuwa, 'Tumekuradhau kwa
namna gani?' Kwa kusema hivyomeza ya Bwana imedharauliwa. 8 Mkitoa sadaka
ya wanyama vipofu, hiyo siyo dhambi? na kama mkitoa vilema na wagonjwa, hiyo
siyo dhambi? pelekeni hili kwa liwali; atawakubali au atainua nyuso zetu?” asema
Bwana wa Majeshi. 9 Na sasa, mnajaribu kutafuta neema ya Mungu, ili kwamba awe
mwema kwetu. “Na aina gani ya sadaka kwa sehemu yenu, ataziinua nyuso zenu?
asema Bwana wa Majeshi. 10 Kama kungekuwa na mtu ambaye angefunga lango la
Hekalu, ili kwamba kusewe na mto madhabahuni bure! lakini sina radhi na ninyi,
“ asema Bwana wa majeshi, “na sitaikubali sadaka yeyote kutoka katika mikono
yenu. 11 Kutoka mawio ya jua mpaka machweo jina langu litakuwa kuu katikati
ya mataifa; katika kila sehemu uvumba utatolewa katika jina langu, na pia sadaka
safi. Kwa sababu jina langu likuwa kuu sana katikatik ya mataif,” asema Bwana
wa majeshi. 12 “lakini ninyi mnachafua mnaposema meza ya Bwana mnainajisi, na
matunda yake, na chakula chake kudharauka. 13 Na ninyi pia mwasema, 'jambo
hili limetuchosha, nanyi mnalidharau, “ asema Bwana wa majeshi. “Mmerudisha
kilichokuwa kimechukuliwa na wanyama wa mwitu au vilema au walio wagonjwa;
na ndicho mnaleta kuwa sadaka zenu! Je naweza kuikubali hii mikononi mwenu?”
asema Bwana. 14 Alaniwe alye mdanganyifu, ambaye anaye mnyama dume katika
kundi lake ana akaahidi kunitolea, lakini bado anatoa kwangu, mimi Bwana, ambayo
ni kiujanja ujanja; kwa kuwa mimi ni mfalme mkuu,” asema Bwana wa Majeshi, “na
jina langu litaogopwa katika mataifa.”

## 2

1 Sasa, ninyi makuhani, amri hii ni kwa ajili yenu. 2 Kama hamtasikiliza, na kama
hamtalichukua hili mioyoni mwenu na kunipa utukufu kwa jina langu, “ asema
Bwana wa Majeshi, Kisha nitatuma laana kwenu, na nitalaani baraka zenu. Kiukweli,
nilishawalaani tayari, kwa sababu hujaweka sheria zangu moyoni. 3 Tazama,
nitakikemea kizazi chako, na nitapaka mavi juu ya uso wako, mavi ya dhabihu zenu,
na mtachukuliwa pamoja nayo. 4 Na mtajua kwamba nimetuma hii sheria kwenu,
kwamba agano langu litakuwa ni juu yangu na Lawi,” asema Bwana wa Majeshi.
5 Agano langu na yeye lilikuwa agano la uhai na amani, na nilimpa vitu hivi kama
njia ya kuniheshimu. aliniheshima na alisimama akawa na hofu kwa jina langu.
6 Mafundisho ya kweli yalikuwa kwenye kinywa chake, na uovu haukupatikana
kinywani mwake. Alitembea na mimi kwa amani na unyoofu, na aliwarudisha wengi

kutoka dhambini. [7] kwa sababu midomo ya makuhani huhifadhi maarifa, na watu
watatafuta maagizo kutoka kwenye kichwa chake, kwa sababu ni mjumbe wa Bwana
wa Majeshi. [8] lakini umepita mbali na njia ya kweli. Umesababisha wengi kuwa na
mashaka ya kutii sheria. umeliharifu agano la Lawi," asema Bwana wa Majeshi.
[9] Kwa hiyo nimewafanya ninyi nanyi kudharauliwa mbele ya watu, kwa sababu
hamkutunza njia zangu, lakini badala yake mnapendelea katika maagizo yenu. [10] Sisi
sote hatuna baba mmoja? Siyo Mungu yule mmoja aliyetuumba sote? kwa nini
tunafanyiana hila kila mtu na ndugu yake, mnariharibu agano la baba zetu? [11] Yuda
amefanya hila na ameona kinyaa kwa vitu vilivyowekwa katika Israeli na Yerusalem.
Yuda amenajisi mahali patakatifu pa Bwana ambapo anapapenda, na ameoa binti wa
miungu migeni. [12] Mungu akukatilie mbali kutoka kwenye hema ya Yakobo na uzao
wa mtu aliyefanya haya, hata yule anayeleta sadaka kwa Bwana wa Majeshi. [13] Na
wewe pia fanya hivyo. Unafunika madhabahu ya Bwana kwa machozi, kwa kilio
na kuugua, kwa sababu hatakubali sadaka na kuzipokea kutoka mikononi mwako.
[14] Lakini wasema, ni kwa sababu gani?" Kwa sababu Bwana amekuwa shahidi kati
yako wewe na mke wako wa ujana wako, kinyume chake umekuwa si mwaminifu,
ingawa yeye ni mwenzako na mke wa agano lako. [15] Je yeye hakuwafanya kuwa
mmoja, hata kwa sehemu ya roho yake? Sasa ni kwanini aliwafanya ninyi kuwa
mmoja? Kwa sababu alikuwa anategemea kupata watoto wacha Mungu. Kwa hiyo
jiepushe mwenyewe ndani ya moyo wako, na asiwepo mtu asiye mwaminifu kwa
mke wa ujana wake. [16] "Nakuchukia kuachana," asema Bwana, Mungu wa Israel,
"afunikizaye nguo yake kwa udhalimu," asema Bwana wa Majeshi. "Kwa hiyo jilinde
ewe mwenyewe ndani ya roho yako na usiwe mtu asiye mwaminifu." [17] Mmechosha
Bwana na maneno. Lakini mwasema, "Tumekuchoshaje?" Kwa kusema Kila mmoja
aliyefanya uovu ni mzuri kwa upande wa Bwana, na anafuraha nao;" au "Yuko wapi
Mungu wa Haki?"

# 3

[1] Tazama, namtuma mjumbe wangu, atakayeandaa njia mbele yangu. Na Bwana,
ambaye mnamtafuta, atakuja ghafla katika hekalu lake; na mjumbe wa agano,
ambaye katika yeye mnafurahi, tazama anakuja." asema Bwana wa Majeshi. [2] Na
ni nani atakeyevumilia siku ya kuja kwake? na nani atasimama akishatokea?
Yeye ni kama mtu asafishaye kwa moto na kama sabuni ya kufulia. [3] Atakaa na
kutawala kama msafishaji wa fedha, na atawasafisha wana wa Lawi. na atawafanya
wawe safi kama dhahabu na fedha, na wataleta sadaka za haki kwa Bwana. [4] Na
sadaka ya Yuda na Yerusalem itampendeza Bwana, kama siku za kale, na miaka ya
zamani. [5] Kisha nitapita karibu na ninyi kuwahukumu. na nitakuwa shahidi mwepesi
dhidi ya wachawi, wazinzi, mahsahidi wa uongo, na kinyume cha wale wanaoonea
wafanyakazi katika mizigo yake, wanaoonea wajane na yatima, na anayemfukuza
mgeni kutoka kwenye haki yake, na kwa wale wasionitii mimi,"asema Bwana
wa majeshi. [6] Mimi Bwana, sibadiliki; pia ninyi, watu wa Yakobo, hamkutumia.
[7] Toka siku za baba zenu mmegeukia mbali na amri zangu na hamkuzitunza.
Nigeukieni, nami nitawarudia ninyi," asema Bwana wa majeshi. Lakini mwasema,
tutakurudiaje? [8] Mwanadamu anaweza kumwibia Mungu? Mnaniibia mimi, lakini
mwasema, 'Tumekuibiaje?' kwa zaka na sadaka. [9] Mmelaani kwa laana, kwa kuniibia
mimi, taifa lote hili. [10] Leteni zaka kamili katika ghalani, ili kwamba kiwemo
chakula katika nyumba yangu. Na mnijaribu kwa hili," asema Bwana wa Majeshi.
"kama sitawafungulia madilisha ya mbinguni na kuwamwagia baraka juu yenu, ili
kwamba hakutakuwa na sehemu ya kutosha kuzipokea. [11] Nitamkemea mharibifu
kwako, kwamba asiharibu mavuno yenu ya nchi yenu; mizazibu yenu katika shamba

haitapukutisha kabla ya wakati wake,” asema Bwana wa Majeshi. 12 Mataifa
yote watakuita mbarikiwa; kwa ajili yako itakuwa ni nchi ya furaha,” asema
Bwana wa Majeshi. 13 Maneo yenu yamekuwa magumu kinyume changu,” asema
Bwana. lakini mwasema, “Tumesema nini kinyume chako?' 14 mmesema, 'Hakuna
maana kumtumikia Mungu. Kuna faida ya namna gani kutunza maagizo yake au
kutembea huku mkiomboleza mbele za Bwana wa Majeshi? 15 Na sasa tunamwita
mwenye kiburi mbarikiwa. Waharifu si kufanikiwa tu, bali kumjaribu Mungu
na kumwepuka.” 16 Kisha wale wanaomweshimu Bwana walisemezana mmoja
baada ya mwingine; Bwana yuko makini kutusikiliza, na kitabu cha kumbukumbu
kiliandikwa mbele zake kwa ajili ya wale wanamwogopa Bwana na kuliheshimu jina
lake. 17 “Watakuwa wangu,” asema Bwana wa majeshi,” hazina zangu, katika siku
nitakayotenda; nitawapenda, kama mtu anavyompenda mwanawe anayemhudumia.
18 Kisha zaidi sana nitatofautisha kati ya haki wenye haki na waovu, kati ya
anayemwabudu Mungu na asiyemwabudu yeye.

# 4

1 Tazama, siku inakuja, inaka kama tanuru, ambayo wote wenye kiburi na waharifu
watakuwa mabua. siku inakuja itawachoma,” asema Bwana wa Majeshi, “siku
hiyo itaondoa mzizi au shina. 2 Lakini kwenu mnaoliogopa jina langu, jua la haki
litawaangazia na uponyaji katika mbawa zake. Mtarukaruka kama ndama zizini.
3 Na waovu wote mtawakanyaga chini, watakuwa majivu chini ya nyazo za miguu
yenu siku hiyo nitatenda,”asema Bwana wa Majeshi. 4 Kumbukeni kutii sheria za
mtumishi wangu Musa, mmri na sheria nilizomwamuru huko Horebu, kwa Israel
wote. 5 Tazama, nitamtuma Eliya nabii mbele ya siku kuu na yenye kutisha ya kuja
kwa Bwana. 6 Atarudisha moyo wa baba kwa watoto, na mioyo ya watoto kwa baba
zao; ili kwamba nisije nikaiangamiza nchi kwa uharibifu wote.”

# Mathayo

1 Kitabu cha ukoo wa Yesu Kristo mwana wa Daudi, mwana wa Ibrahimu.
2 Ibrahimu alikuwa baba wa Isaka, na Isaka baba wa Yakobo, na Yakobo baba
wa Yuda na ndugu zake. 3 Yuda alikuwa baba wa Peresi na Sera kwa Tamari,
Peresi baba wa Hezeroni, na Hezeroni baba wa Ramu. 4 Ramu alikuwa baba wa
Aminadabu, Aminadabu baba wa Nashoni, na Nashoni baba wa Salimoni. 5 Salimoni
alikuwa baba wa Boazi kwa Rahabu, Boazi baba wa Obedi kwa Ruth, Obedi baba
wa Yese, 6 Yese alikuwa baba wa mfalme Daudi. Daudi alikuwa baba wa Sulemani
kwa mke wa Uria. 7 Sulemani alikuwa baba wa Rehoboamu, Rehoboamu baba wa
Abiya, Abiya baba wa Asa. 8 Asa alikuwa baba wa Yehoshafati, Yehoshafati baba wa
Yoramu, na Yoramu baba wa Uzia. 9 Uzia alikuwa baba wa Yothamu, Yothamu baba
wa Ahazi, Ahazi baba wa Hezekia. 10 Hezekia alikuwa baba wa Manase, Manase
baba wa Amoni na Amoni baba wa Yosia. 11 Yosia alikuwa baba wa Yekonia na
kaka zake wakati wa kuchukuliwa kwenda Babeli. 12 Na baada ya kuchukuliwa
kwenda Babeli, Yekonia alikuwa baba wa Shatieli, Shatieli alikuwa babu yake na
Zerubabeli. 13 Zerubabeli alikuwa baba wa Abiudi, Abiudi baba wa Eliakimu, na
Eliakimu baba wa Azori. 14 Azori alikuwa baba wa Zadoki, Zadoki baba wa Akimu,
na Akimu baba wa Eliudi. 15 Eliudi alikuwa baba wa Elieza, Elieza baba wa Matani
na Matani baba wa Yakobo. 16 Yakobo alikuwa baba wa Yusufu mume wa Mariamu,
ambaye kwa yeye Yesu alizaliwa, aitwaye Kristo. 17 Vizazi vyote tangu Ibrahimu
hadi Daudi vilikuwa vizazi kumi na vinne, kutoka Daudi hadi kuchukuliwa kwenda
Babeli vizazi kumi na vinne, na kutoka kuchukuliwa kwenda Babeli hadi Kristo vizazi
kumi na vinne. 18 Kuzaliwa kwa Yesu Kristo kulikuwa kwa namna hii. Mama yake,
Mariamu, alichumbiwa na Yusufu, lakini kabla hawajakutana, alionekana kuwa na
mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. 19 Mume wake Yusufu, alikuwa mtu mwenye
haki hakutaka kumwaibisha hadharani. Aliamua kusitisha uchumba wake naye kwa
siri. 20 Alipokuwa akifikiri juu ya mambo haya, Malaika wa Bwana alimtokea katika
ndoto, akisema,'' Yusufu mwana wa Daudi, usiogope kumchukua Mariamu kama
mkeo, kwa sababu mimba aliyonayo ni kwa uweza wa Roho Mtakatifu. 21 Atajifungua
mtoto wa kiume na utamwita jina lake Yesu, kwa maana atawaokoa watu wake na
dhambi zao.'' 22 Yote haya yalitokea kutimizwa kile kilichonenwa na Bwana kwa njia
ya nabii, akisema, 23 “Tazama, bikira atachukua mimba na kuzaa mtoto wa kiume,
na watamwita jina lake Imanueli”— maana yake, “Mungu pamoja nasi.” 24 Yusufu
aliamka kutoka usingizini na kufanya kama malaika wa Bwana alivyomwamuru na
alimchukua kama mkewe. 25 Hata hivyo, hakulala naye mpaka alipojifungua mtoto
wa kiume na alimwita jina lake Yesu.

## 2

1 Baada ya Yesu kuzaliwa katika Bethelehem ya Uyahudi katika siku za mfalme
Herode, watu wasomi kutoka mashariki ya mbali walifika Yerusalemu wakisema,
2 “Yuko wapi yeye ambaye aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi? Tuliiona nyota yake
mashariki nasi tumekuja kumwabudu.” 3 Pindi Mfalme herode aliposikia haya
alifadhaika, na Yerusalemu yote pamoja naye. 4 Herode akawakusanya wakuu
wa makuhani wote na waandishi wa watu, naye akawauliza, “Kristo atazaliwa
wapi?” 5 Wakamwabia, “Katika Bethelehemu ya Uyahudi, kwa kuwa hivi ndivyo
ilivyoandikwa na nabii, 6 Nawe Bethelehemu, katika nchi ya Yuda, si mdogo miongoni
mwa viongozi wa Yuda, kwa kuwa kutoka kwako atakuja mtawala atakayewachunga
watu wangu Israeli.” 7 Hivyo Herode aliwaita wale wasomi kwa siri na kuwauliza ni

wakati gani hasa nyota ilikuwa imeonekana. 8 Akawatuma Bethelehem, akisema,
“Nendeni kwa uangalifu mkamtafute mtoto aliyezaliwa. Wakati mtakapomwona,
nileteeni habari ili kwamba mimi pia niweze kuja na kumwabudu.” 9 Baada ya
kuwa wamemsikia mfalme, waliendelea na safari yao, na nyota ile waliyokuwa
wameiona mashariki iliwatangulia hadi iliposimama juu ya mahali mtoto aliyezaliwa
alipokuwa. 10 Wakati walipoiona nyota, walifurahi kwa furaha kuu mno. 11 Waliingia
nyumbani na kumuona mtoto aliyezaliwa na Mariamu mama yake. Walimsujudia na
kumwabudu. Walifungua hazina zao na kumtolea zawadi za dhahabu, uvumba, na
manemane. 12 Mungu aliwaonya katika ndoto wasirudi kwa Herode, hivyo, walion-
doka kurudi katika nchi yao kwa njia nyingine. 13 Baada ya kuwa wameondoka,
malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto na kusema, “Inuka, mchukue
mtoto na mama yake na mkimbilie Misri. Bakini huko mpaka nitakapowaambia,
kwa kuwa Herode atamtafuta mtoto ili amwangamize. 14 Usiku huo Yusufu aliamka
na kumchukua mtoto na mama yake na kukimbilia Misri. 15 Aliishi huko hadi Herode
alipo kufa. Hii ilitimiza kile Bwana alichokuwa amenena kupitia nabii, “Kutoka Misri
nimemwita mwanangu.” 16 Kisha Herode, alipoona kuwa amedhihakiwa na watu
wasomi, alikasirika sana. Aliagiza kuuawa kwa watoto wote wa kiume waliokuwa
Bethelehemu na wote katika eneo lile ambao walikuwa na umri wa miaka miwili
na chini yake kulingana na wakati aliokuwa amekwisha thibitisha kabisa kutoka
kwa wale watu wasomi. 17 Ndipo lilipotimizwa lile neno lililonenwa kwa kinywa
cha nabii Yeremia, 18 “Sauti ilisikika Ramah, kilio na maombolezo makubwa, Raheli
akiwalilia watoto wake, na alikataa kufarijiwa, kwa sababu hawapo tena.” 19 Herode
alipo kufa, tazama malaika wa Bwana alimtokea Yusufu katika ndoto huko Misri na
kusema, 20 “Inuka mchukue mtoto na mama yake, na mwende katika nchi ya Israeli
kwa maana waliokuwa wakitafuta uhai wa mtoto wamekufa.” 21 Yusufu aliinuka,
akamchukua mtoto pamoja na mama yake, na wakaja katika nchi ya Israeli. 22 Lakini
aliposikia kuwa Arikelau alikuwa anatawala Yuda mahali pa baba yake Herode,
aliogopa kwenda huko. Baada ya Mungu kumuonya katika ndoto, aliondoka kwenda
mkoa wa Galilaya 23 na alienda kuishi katika mji uitwao Nazareti. Hili lilitimiza kile
kilichokuwa kimekwisha kunenwa kwa njia ya manabii, kwamba ataitwa Mnazareti.

# 3

1 Katika siku zile Yohana Mbatizaji alikuja akihubiri katika nyika ya Yuda akisema,
2 “Tubuni kwa maana ufalme wa mbinguni u karibu.” 3 Kwa maana huyu ndiye
aliyenenwa na nabii Isaya akisema, “sauti ya mtu aitaye kutoka jangwani; 'wekeni
tayari njia ya Bwana, yanyoosheni mapito yake.”' 4 Sasa Yohana alivaa manyoya
ya ngamia na mkanda wa ngozi kiunoni mwake. Chakula chake kilikuwa nzige na
asali ya mwituni. 5 Kisha Yerusalemu, Yuda yote, na eneo lote linalozunguka mto
Yorodani wakaenda kwake. 6 Walikuwa wakibatizwa naye katika mto Yorodani huku
wakitubu dhambi zao. 7 Lakini alipowaona wengi wa mafarisayo na masadukayo
wakija kwake kubatizwa, akawaambia, ''Enyi uzao wa nyoka wenye sumu nani
aliye waonya kuikimbia ghadhabu inayokuja? 8 Zaeni matunda yaipasayo toba.
9 Na msifikiri na kusemezana miongoni mwenu, 'Tunaye Ibrahimu kama baba yetu.'
Kwa kuwa nawaambieni Mungu anaweza kumwinulia Ibrahimu watoto hata kutoka
katika mawe haya. 10 Tayari shoka limekwisha kuwekwa kwenye mzizi wa miti.
Kwahiyo kila mti usiozaa matunda mazuri hukatwa na kutupwa kwenye moto.
11 Ninawabatiza kwa maji kwa ajili ya toba. Lakini yeye ajaye baada yangu ni
mkuu kuliko mimi nami sistahili hata kubeba viatu vyake. Yeye atawabatiza kwa
Roho Mtakatifu na kwa moto. 12 Na pepeto lake li mkononi mwake kusafisha kabisa
uwanda wake na kuikusanya ngano yake ghalani. Lakini atayachoma makapi kwa

moto ambao hauwezi kuzimika. 13 Kisha Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka mto
Yorodani kubatizwa na Yohana. 14 Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, “Mimi
nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu?'' 15 Yesu akajibu akasema, ''Ruhusu
iwe hivi sasa, kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote.'' Kisha Yohana
akamruhusu. 16 Baada ya kuwa amebatizwa, mara Yesu alitoka kwenye maji, na
tazama, Mbingu zikafunguka kwake. Na alimuona Roho wa Mungu akishuka kwa
mfano wa njiwa na kutulia juu yake. 17 Tazama, sauti ilitoka mbinguni ikisema,
“Huyu ni mwanangu mpendwa. Ninaye pendezwa sana naye.''

# 4

1 Kisha Yesu aliongozwa na Roho mpaka jangwani ili ajaribiwe na ibilisi.
2 Alipokuwa amefunga kwa siku arobaini mchana na usiku alipata njaa. 3 Mjarabu
akaja na akamwambia, “Kama wewe ni Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe
mkate.” 4 Lakini Yesu alimjibu na kumwambia, “Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa
mkate peke yake, bali kwa kila neno litokalo kinywani mwa Mungu.''' 5 Kisha ibilisi
akampeleka katika mji mtakatifu na kumweka mahali pa juu sana pa jengo la hekalu,
6 na kumwambia,'' kama wewe ni Mwana wa Mungu, jirushe chini, kwa maana
imeandikwa, 'Ataamuru malaika wake waje wakudake,' na, 'watakuinua kwa mikono
yao, ili usijikwae mguu wako katika jiwe.” 7 Yesu akamwambia, ''Tena imeandikwa,
'Usimjaribu Bwana Mungu wako.''' 8 Kisha, ibilisi akamchukua na kumpeleka sehemu
ya juu zaidi akamwonyesha falme zote za ulimwengu na fahari ya hizo zote.
9 Akamwambia, “Nitakupa vitu vyote hivi ukunisujudia na kuniabudu.” 10 Kisha
Yesu akamwambia, “Nenda zako utoke hapa, Shetani! Kwa maana imeandikwa,
'Yakupasa kumwabudu Bwana Mungu wako, na umtumikie yeye peke yake.'” 11 Kisha
ibilisi akamwacha, na tazama, malaika wakaja wakamtumikia. 12 Basi Yesu aliposikia
kuwa Yohana amekamatwa, aliondoka mpaka Galilaya. 13 Aliondoka Nazareti alienda
na kuishi Kaperanaumu, iliyoko kandokando na Bahari ya Galilaya, mipakani mwa
majimbo ya Zabuloni na Naftali. 14 Hii ilitokea kutimiza kile kilichonenwa na nabii
Isaya, 15 “Katika mji wa Zabuloni na mji wa Naftali, kuelekea Baharini, ng'ambo
ya Yorodani, Galilaya ya wamataifa! 16 Watu walio kaa gizani wameuona mwanga
mkuu, na wale waliokuwa wameketi katika maeneo na kivuli cha mauti, juu yao
nuru imewaangazia.'' 17 Tokea wakati huo Yesu alianza kuhubiri na kusema, “Tubuni,
kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia.'' 18 Alipokuwa akitembea kandokando
ya Bahari ya Galilaya, aliwaona ndugu wawili, Simoni aliyekuwa akiitwa Petro, na
Andrea kaka yake, wakitega nyavu baharini, kwa kuwa walikuwa wavuvi wa samaki.
19 Yesu akawaambia, “Njooni mnifuate, nitawafanya kuwa wavuvi wa watu.” 20 Mara
moja waliziacha nyavu na walimfuata. 21 Na Yesu alipokuwa akiendelea kutoka
hapo aliwaona ndugu wawili wengine, Yakobo mwana wa Zebedayo, na Yohana kaka
yake. Walikuwa katika mtumbwi pamoja na Zebedayo baba yao wakishona nyavu
zao. Akawaita, 22 na mara moja wakaacha mtumbwi na baba yao nao wakamfuata.
23 Yesu alienda karibia Galilaya yote, akifundisha katika Masinagogi yao, akihubiri
injili ya ufalme, na akiponya kila aina ya maradhi na magonjwa miongoni mwa watu.
24 Habari zake zilienea Siria yote, na watu wakawaleta kwake wale wote waliokuwa
wakiugua, wakiwa na maradhi mbalimbali na maumivu, waliokuwa na mapepo, na
wenye kifafa na waliopooza. Yesu aliwaponya. 25 Umati mkubwa wa watu ulimfuata
kutoka Galilaya, na Dekapoli, na Yerusalemu na Uyahuda na kutoka ng'ambo ya
Yorodani.

# 5

1 Yesu alipo uona umati, akaondoka na kuelekea Mlimani. Alipokuwa ameketi

chini, wanafunzi wake wakaja kwake. 2 Akafunua kinywa chake na akawafundisha,
akisema, 3 “Heri walio maskini wa roho maana ufalme wa mbinguni ni wao. 4 Heri
walio na huzuni, maana watafarijiwa. 5 Heri wenye upole, maana watairithi nchi.
6 Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa. 7 Heri wenye rehema
maana hao watapata Rehema. 8 Heri wenye moyo safi maana watamwona Mungu.
9 Heri wapatanishi, maana hao wataitwa wana wa Mungu. 10 Heri wale wanaoteswa
kwa ajili ya haki, maana ufalme wa mbinguni ni wao. 11 Heri ninyi ambao watu
watawatukana na kuwatesa, au kusema kila aina ya ubaya dhidi yenu kwa uongo
kwa ajili yangu. 12 Furahini na kushangilia, maana thawabu yenu ni kubwa juu
mbinguni. Kwa kuwa hivi ndivyo watu walivyo watesa manabii walioishi kabla
yenu. 13 Ninyi ni chumvi ya dunia. Lakini kama chumvi imepoteza ladha yake,
itawezaje kufanyika chumvi halisi tena? Kamwe haiwezi kuwa nzuri kwa kitu
kingine chochote tena, isipokuwa ni kutupwa nje na kukanyagwa na miguu ya watu.
14 Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji uliojegwa juu ya mlima haufichiki. 15 Wala watu
hawawashi taa na kuweka chini ya kikapu, bali kwenye kinara, nayo yawaangaza
wote walio ndani ya nyumba. 16 Acha nuru yenu iangaze mbele za watu kwa namna
ambayo kwamba, wayaone matendo yenu mema na kumtukuza Baba yenu aliye
mbinguni. 17 Msifikiri nimekuja kuiharibu sheria wala manabii. Sijaja kuharibu
lakini kutimiza. 18 Kwa kweli nawaambia kwamba mpaka mbingu na dunia zote
zipite hapana yodi moja wala nukta moja ya sheria itaondoshwa katika sheria hadi
hapo kila kitu kitakapokuwa kimekwisha timizwa. 19 Hivyo yeyote avunjaye amri
ndogo mojawapo ya amri hizi na kuwafundisha wengine kufanya hivyo ataitwa
mdogo katika ufalme wa mbinguni. Lakini yeyote azishikaye na kuzifundisha ataitwa
mkubwa katika ufalme wa mbinguni. 20 Kwa maana nawaambia haki yenu isipozidi
haki ya waandishi na Mafarisayo, kwa vyovyote vile hamtaingia katika ufalme wa
mbinguni. 21 Mmesikia ilinenwa zamani kuwa, “usiue” na 'yeyote auaye yuko katika
hatari ya hukumu.' 22 Lakini nawaambia yeyote amchukiaye ndugu yake atakuwa
katika hatari ya hukumu. Na yeyote amwambiaye ndugu yake kuwa, 'Wewe ni mtu
usiyefaa!' atakuwa katika hatari ya baraza. Na yeyote asemaye, 'Wewe mjinga!'
atakuwa katika hatari ya moto wa jehanamu. 23 Hivyo kama unatoa sadaka yako
katika madhabahu na unakumbuka kuwa ndugu yako ana jambo lolote dhidi yako,
24 iache sadaka mbele ya madhabahu, kisha shika njia yako. Kapatane kwanza na
ndugu yako, na kisha uje kuitoa sadaka yako. 25 Patana na mshitaki wako upesi,
ukiwa pamoja naye njiani kuelekea mahakamani, vinginevyo mshtaki wako anaweza
kukuacha mikononi mwa hakimu, na hakimu akuache mikononi mwa askari, nawe
utatupwa gerezani. 26 Amini nawaambieni, kamwe hutawekwa huru hadi umelipa
senti ya mwisho ya pesa unayodaiwa. 27 Mmesikia imenenwa kuwa, 'Usizini.'
28 Lakini nawaambieni yeyote amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha
kuzini naye moyoni mwake. 29 Na kama jicho lako la kulia linakusababisha kujikwaa,
ling'oe na ulitupe mbali nawe. Kwa kuwa ni afadhali kiungo kimoja katika mwili
wako kiharibike kuliko mwili mzima kutupwa jehanamu. 30 Na kama mkono wako
wa kuume unakusababisha kujikwaa, ukate kisha uutupilie mbali nawe. Maana ni
afadhali kiungo kimoja katika mwili wako kiharibike kuliko mwili mzima kutupwa
jehanamu. 31 Imenenwa pia, yeyote amfukuzaye mkewe, na ampe hati ya talaka.'
32 Lakini mimi nawaambia, yeyote anaye mwacha mke wake, isipokuwa kwa kwa
sababu ya zinaa, amfanya kuwa mzinzi. Na yeyote amuoaye baada ya kupewa talaka
afanya uzinzi. 33 Tena, mmesikia ilinenwa kwa wale wa zamani, 'Msiape kwa uongo,
bali pelekeni viapo vyenu kwa Bwana.' 34 Lakini nawaambia, msiape hata kidogo,
ama kwa mbingu, kwa sababu ni enzi ya Mungu; 35 wala kwa dunia, maana ni mahali
pa kuweka kiti cha kukanyagia nyayo zake, ama kwa Jerusalemu, maana ni mji wa

mfalme mkuu. [36] Wala usiape kwa kichwa chako, maana huwezi kufanya unywele
mmoja kuwa mweupe au mweusi. [37] Bali maneno yenu yawe, 'Ndiyo, ndiyo, Hapana,
hapana.' Kwa kuwa yazidiyo hayo yatoka kwa yule mwovu. [38] Mmesikia imenenwa
kuwa, 'Jicho kwa jicho, na jino kwa jino.' [39] Lakini mimi namwambia, Msishindane na
mtu mwovu; lakini mtu akikupiga shavu la kulia mgeuzie na jingine pia. [40] Na kama
yeyote anatamani kwenda na wewe mahakamani na akakunyang'anya kanzu yako,
mwachie na joho lako pia. [41] Na yeyote akulazimishaye kwenda naye maili moja,
nenda naye maili mbili. [42] Kwa yeyote akuombaye mpatie, na usimwepuke yeyote
anayehitaji kukukopa. [43] Mmesikia imenenwa, 'Umpende jirani yako, na umchukie
adui yako.' [44] Lakini nawaambia, wapendeni adui zenu, waombeeni wanao waudhi,
[45] Ili kwamba muwe watoto wa baba yenu aliye mbinguni. Kwa kuwa anafanya jua
liwaangazie wabaya na wema, na anawanyeshea mvua waovu na wema. [46] Kama
mkiwapenda wanaowapenda ninyi, mwapata thawabu gani? Kwani watoza ushuru
hawafanyi hivyo? [47] Na kama mkiwasalimia ndugu zenu tu mwapata nini zaidi ya
wengine? Je!, Watu wa mataifa hawafanyi vivyo hivyo? [48] Kwa hiyo yawapasa kuwa
wakamilifu, kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.

# 6

[1] Zingatia kutotenda matendo ya haki mbele ya watu ili kujionyesha, vinginevyo
hutapata thawabu kutoka kwa Baba aliye mbinguni. [2] Hivyo basi unapotoa usipige
tarumbeta na kujisifu mwenyewe kama wanafiki wanavyofanya katika masinagogi
na katika mitaa, ili kwamba watu wawasifu. Kweli nawaambia, wamekwisha
kupokea thawabu yao. [3] Lakini wewe unapotoa, mkono wako wa kushoto usijue
kinachofanywa na mkono wa kulia, [4] ili kwamba zawadi yako itolewe kwa siri. Ndipo
Baba yako aonaye sirini atakupatia thawabu yako. [5] Na unapokuwa ukiomba, usiwe
kama wanafiki, kwa kuwa wanapenda kusimama na kuomba kwenye masinagogi
na kwenye kona za mitaani, ili kwamba watu wawatazame. Kweli nawaambia,
wamekwishapokea thawabu yao. [6] Lakini wewe, unapo omba, ingia chumbani.
Funga mlango, na uombe kwa kwa Baba yako aliye sirini. Ndipo Baba yako aonaye
sirini atakupatia thawabu yako. [7] Na unapokuwa ukiomba, usirudie rudie maneno
yasiyo na maana kama mataifa wanavyofanya, kwa kuwa wanafikiri kwamba
watasikiwa kwa sababu ya maneno mengi wanayosema. [8] Kwa hiyo, usiwe kama
wao, kwa kuwa Baba yako anatambua mahitaji yako hata kabla hujaomba kwake.
[9] Hivyo basi omba hivi: Baba yetu uliye mbinguni, ulitukuze jina lako. [10] Ufalme
wako uje, mapenzi yako yafanyike hapa duniani kama huko mbinguni. [11] Utupatiye
leo mkate wetu wa kila siku. [12] utusamehe deni zetu, kama nasi tunavyowasamehe
wadeni wetu. [13] Na usitulete katika majaribu, lakini utuepushe kutoka kwa yule
mwovu.' [14] Ikiwa mtawasemehe watu makosa yao, Baba yako aliye mbinguni pia
atawasamehe ninyi. [15] Lakini ikiwa hamtawasamehe makosa yao, wala Baba yenu
hatawasamehe makosa yenu. [16] Zaidi ya yote, unapokuwa umefunga, usioneshe
sura ya huzuni kama wanafiki wanavyofanya, kwa kuwa wanakunja sura zao ili
kwamba watu wawatambue wamefunga. Kweli ninakuambia, wamekwisha kupokea
thawabu yao. [17] Lakini wewe, unapokuwa umefunga, paka mafuta kichwa chako na
uoshe uso wako. [18] Hivyo haitakuonesha mbele ya watu kuwa umefunga, lakini tu
itakuwa kwa Baba yako aliye sirini. Na Baba yako aonaye sirini, atakupa thawabu
yako. [19] Usijitunzie hazina yako mwenyewe hapa duniani, ambapo nondo na kutu
huharibu, ambapo wezi huvunja na kuiba. [20] Badala yake, jitunzie hazina yako
mwenyewe mbinguni, ambapo wala nondo wala kutu hawezi kuharibu, na ambapo
wezi hawawezi kuvunja na kuiba. [21] Kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo na moyo
wako utakapokuwepo pia. [22] Jicho ni taa ya mwili. Kwa hiyo, ikiwa jicho lako

ni zima, mwili wote utajazwa na nuru. 23 Lakini ikiwa jicho lako ni bovu, mwili
wako wote umejaa giza totoro. Kwahiyo, ikiwa nuru ambayo imo ndani yako ni
giza hasa, ni giza kubwa kiasi gani! 24 Hakuna hata mmoja anayeweza kuwatumikia
mabwana wawili, kwa kuwa atamchukia mmoja na kumpenda mwingine, au la sivyo
atajitoa kwa mmoja na kumdharau mwingine. Hamuwezi kumtumikia Mungu na
mali. 25 Kwa hiyo nakuambia, usiwe na mashaka kuhusu maisha yako, kuwa utakula
nini au utakunywa nini, au kuhusu mwili wako, utavaa nini. Je! Maisha si zaidi ya
chakula na mwili zaidi ya mavazi? 26 Tazama ndege walioko angani. Hawapandi
na hawavuni na hawakusanyi na kutunza ghalani, lakini Baba yenu wa mbinguni
huwalisha wao. Je ninyi si wa thamani zaidi kuliko wao? 27 Na ni nani miongoni
mwenu kwa kujihangaisha anaweza kuongeza dhiraa moja kwenye uhai wa maisha
yake? 28 Na kwa nini mna kuwa na wasiwasi kuhusu mavazi? Fikiria kuhusu maua
kwenye mashamba, jinsi yanavyokua. Hayafanyi kazi na hayawezi kujivisha. 29 Bado
ninawaambia, hata Sulemani katika utukufu wake wote hakuvikwa kama mojawapo
ya haya. 30 Ikiwa Mungu anayavalisha majani katika mashamba, ambayo yadumu
siku moja na kesho yanatupwa katika moto, je ni kwa kiasi gani atawavalisha ninyi,
ninyi wenye imani ndogo? 31 Kwa hiyo msiwe na wasiwasi nakusema, 'Je tutakula
nini?' au "Je tutakunywa nini?" au "Je tutavaa nguo gani?" 32 Kwa kuwa mataifa
wanatafuta mambo haya, na Baba yenu wa mbinguni anajua kuwa mnahitaji hayo.
33 Lakini kwanza tafuteni ufalme wake na haki yake na haya yote yatakabidhiwa
kwako. 34 Kwa hiyo, usione shaka kwa ajili ya kesho, kwa kuwa kesho itajishughulikia
yenyewe. Kila siku inatosha kuwa na tatizo lake yenyewe.

# 7

1 Usihukumu, nawe usije ukahukumiwa. 2 Kwa hukumu unayohukumu, nawe
utahukumiwa. Na kwa kipimo unachopima na wewe pia utapimiwa hicho hicho.
3 Na kwa nini unatazama kipande cha mti kilichoko kwenye jicho la ndugu yako,
lakini hutambuwi kipande cha gogo ambalo limo katika jicho lako? 4 Unawezaje
kusema kwa ndugu yako, ngoja nikutolee kipande kilichomo kwenye jicho lako,
wakati kipande cha gogo kimo ndani ya jicho lako? 5 Mnafiki wewe; kwanza toa gogo
lililomo kwenye jicho lako, na ndipo utakapoweza kuona vizuri na kukitoa kipande
cha mti kilichomo kwenye jicho la ndugu yako. 6 Usiwape mbwa kilicho kitakatifu, na
usiwarushie nguruwe lulu mbele yao. Vinginevyo wataviharibu na kuvikanyaga kwa
miguu, na tena watakugeukia wewe na kukurarua vipande vipande. 7 Omba, nawe
utapewa. Tafuta, nawe utapata. Bisha hodi, na wewe utafunguliwa. 8 Kwa yeyote
anayeomba, hupokea. Na kwa yeyote anayetafuta, hupata. Na kwa mtu ambaye
anayebisha hodi, atafunguliwa. 9 Au kuna mtu miongoni mwenu ambaye, ikiwa
mtoto wake amemwomba kipande cha mkate atampa jiwe? 10 Au ikiwa atamwomba
samaki, na yeye atampa nyoka? 11 Kwa hiyo, ikiwa ninyi mlio waovu mnajua kuwapa
watoto wenu zawadi nzuri, Je! Ni kiasi gani zaidi Baba aliye mbinguni atawapa
vitu vizuri wale wanao muomba yeye? 12 Kwa sababu hiyo, unapotaka kufanyiwa
kitu chochote na watu wengine, nawe pia itakupasa kuwafanyia hivyo hivyo wao.
Kwa kuwa hiyo ni sheria na manabii. 13 Ingieni kwa kupitia geti jembamba. Kwa
kuwa geti ni pana na njia ni pana inayoongoza kwenye uharibifu, na kuna watu
wengi wanaopitia njia hiyo. 14 Geti ni jembamba, Geti jembamba ni njia inayongooza
katika uzima na ni wachache wanaoweza kuiona. 15 Jihadhari na manabii wa uongo,
wanaokuja wamevaa ngozi ya kondoo, lakini kweli ni mbweha wakali. 16 Kwa
matunda yao mtawatambua. Je watu wanaweza kuvuna matunda kwenye miba, au
mtini kwenye mbengu ya mbaruti? 17 Kwa jinsi hiyo, kila mti mzuri huzaa matunda
mazuri, lakini mti mbaya huzaa matunda mabaya. 18 Mti mzuri hauwezi kuzaa

matunda mabaya, wala mti mbaya hauwezi kuzaa matunda mazuri. 19 Kila mti
ambao hauzai matunda mazuri utakatwa na kutupwa katika moto. 20 Hivyo basi,
utawatambua kutokana na matunda yao. 21 Si kila mtu aniambiaye mimi, 'Bwana,
Bwana,' ataingia katika ufalme wa mbinguni, bali ni yule pekee atendaye mapenzi
ya Baba yangu aliye mbinguni. 22 Watu wengi wataniambia siku hiyo, 'Bwana,
Bwana, hatukutoa unabii kwa jina lako, hatukutoa mapepo kwa jina lako, na kwa jina
lako tulifanya matendo mengi makuu?' 23 Ndipo nitawaambia wazi, 'sikuwatambua
ninyi! Ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu!' 24 Kwa hiyo, kila mmoja asikiaye
maneno yangu na kutii atafanana na mtu mwenye hekima aliyejenga nyumba yake
juu ya mwamba. 25 Mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, na upepo ukaja na ukaipiga
nyumba hiyo, lakini haikuweza kuanguka chini, kwa kuwa ilikuwa imejengwa juu
ya mwamba. 26 Lakini kila mtu anayesikia neno langu na asilitii, atafananishwa na
mtu mpumbavu aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga. 27 Mvua ikaja, mafuriko
yakaja, na upepo ukaja na kuipiga nyumba hiyo. Na ikaanguka, na uharibifu wake
ukakamilika." 28 Ulifika wakati ambao Yesu alipomaliza kuongea maneno haya,
makutano walishangazwa na mafundisho yake, 29 kwa kuwa alifundisha kama mtu
mwenye mamlaka, na si kama waandishi wao.

# 8

1 Wakati Yesu aliposhuka chini kutoka mlimani, umati mkubwa ulimfuata.
2 Tazama, mkoma alikuja na kusujudu mbele yake, akasema, "Bwana, ikiwa uko
tayari, unaweza kunifanya niwe safi". 3 Yesu akanyoosha mkono wake na kumgusa,
akasema, "Niko tayari. Uwe msafi." Hapo hapo alitakaswa ukoma wake. 4 Yesu
akamwambia, "Angalia kwamba usiseme kwa mtu yeyote. Shika njia yako, na
jioneshe mwenyewe kwa kuhani na utoe zawadi ambayo Musa aliagiza, kwa ajili
ya ushuhuda kwao" 5 Wakati Yesu alipofika Kapernaumu, Jemedari akaja kwake
akamuuliza 6 akisema, "Bwana, mtumishi wangu amelala nyumbani amepooza na
ana maumivu ya kutisha." 7 Yesu akamwambia, "Nitakuja na kumponya". 8 Jemedari
akajibu na kumwambia, "Bwana, mimi si wathamani hata uje na kuingia ndani ya
dari yangu, sema neno tu na mtumishi wangu ataponywa. 9 Kwa kuwa mimi pia
ni mtu niliye na mamlaka, na ninao askari walio chini yangu. Nikisema kwa huyu
"Nenda' na huenda, na kwa mwingine 'Njoo' na yeye huja, na kwa mtumishi wangu,
'Fanya hivi,' na yeye anafanya hivyo" 10 Wakati Yesu aliposikia haya, alishangazwa
na kuwaambia wale waliokuwa wakimfuata, "Kweli ninawaambia, Sijapata kuona
mtu mwenye imani kama huyu katika Israel. 11 Ninawambieni, wengi watakuja
kutoka mashariki na magharibi, wataketi katika meza pamoja na Abrahimu, Isaka,
na Yakobo, katika ufame wa mbinguni. 12 Lakini watoto wa ufalme watatupwa katika
giza la nje, ambapo kutakuwa na kilio na kusaga meno." 13 Yesu akamwambia
Jemadari, "Nenda! Kama ulivyokwisha amini, na itendeke hivyo kwako". Na
mtumishi aliponywa katika saa hiyo. 14 Wakati Yesu alipofika kwenye nyumba ya
Petro, alimwona mama mkwe wake na Petro amelala akiwa mgonjwa wa homa.
15 Yesu akamgusa mkono wake, na homa yake ikamwacha. kisha akaamka akaanza
kumhudumia. 16 Na ilipofika jioni, watu wakamletea Yesu wengi waliotawaliwa na
pepo. Akawafukuza pepo na wale walio wagonjwa akawaponya. 17 Kwa jinsi hii
yalitimia yale yaliyo kwisha kunenwa na Isaya nabii, "Yeye mwenyewe alichukua
magonjwa yetu na alibeba maradhi yetu" 18 Kisha Yesu alipoliona kusanyiko
limemzunguka, alitoa maelekezo ya kwenda upande mwingine wa Bahari ya Galilaya.
19 Kisha mwandishi akaja kwake na kumwambia, "Mwalimu, nitakufuata popote
utakapoenda." 20 Yesu akamwambia, "Mbweha wana mashimo, na ndege wa angani
wana viota, lakini mwana wa Adamu hana sehemu ya kulaza kichwa chake."

21 Mwanafunzi mwingine akamwambia, “Bwana, niruhusu kwanza niende kumzika
baba yangu.” 22 Lakini Yesu akamwambia, “Nifuate, na uwaache wafu wazike
wafu wao.” 23 Yesu alipoingia kwenye mtumbwi, wanafunzi wake wakamfuata
mtumbwini. 24 Tazama, ikainuka dhoruba kuu juu ya bahari, kiasi kwamba mtumbwi
ulifunikwa na mawimbi. Lakini Yesu alikuwa amelala. 25 Wanafunzi wakaja
kwake na kumwamsha wakisema, “Bwana, tuokoe sisi, tunaelekea kufa!” 26 Yesu
akawaambia, “kwa nini mnaogopa, ninyi wenye imani ndogo?” Ndipo akaamka
na kuukemea upepo na bahari. Kisha kukawa na utulivu mkuu, 27 wanaume
wakashikwa na mshangao wakasema, “Huyu mtu niwa namna gani, kwamba hata
pepo na bahari vinamtii yeye?” 28 Wakati Yesu alipokuwa amekuja upande mwingine
wa nchi ya Magadala, wanaume wawili waliotawaliwa na pepo walikutana naye.
Walikuwa wakitokea makaburini na walikuwa wakifanya vurugu sana, kiasi kwamba
hakuna msafiri angeweza kupita njia ile. 29 Tazama, walipaza sauti na kusema,
“Tuna nini cha kufanya kwako, mwana wa Mungu? Umekuja hapa kututesa kabla
ya wakati kufika?” 30 Sasa kundi kubwa la nguruwe lilikuwa likichunga, hapakuwa
mbali sana walipokuwa, 31 pepo waliendelea kulalamika kwa Yesu na kusema. “Ikiwa
utatuamuru kutoka, tupeleke kwenye kundi la nguruwe.” 32 Yesu akawaambia,
“Nendeni!” Pepo wakawatoka na kwenda kwa nguruwe. Na tazama, kundi lote
likashuka kutoka mlimani kuteremkia baharini na lote likafia majini. 33 Wanaume
waliokuwa wakichunga nguruwe walikimbia. Na walipoenda mjini wakaelezea kila
kitu, hususani kilichotokea kwa wanaume waliotawaliwa na mapepo. 34 Tazama, mji
mzima ukaja kukutana na Yesu. Walipomwona, walimsihi aondoke kwenye mkoa
wao.

# 9

1 Yesu akaingia kwenye boti, akavuka na akafika kwenye mji alipokuwa anaishi.
2 Tazama, wakamletea mtu aliyepooza amelazwa kwenye godoro. alipooiona imani
yao, Yesu akamwambia mtu aliyepooza, “Mwanangu, uwe na furaha, Dhambi zako
zimesamehewa” 3 Tazama, Baadhi ya walimu wa sheria wakasemezana wao kwa
wao, “Huyu mtu anakufuru” 4 Yesu akatambua mawazo yao na kusema, “Kwa
nini mnawaza maovu moyoni mwenu? 5 Kipi kilicho rahisi kusema, 'Dhambi zako
zimesamehewa' au kusema, 'Simama na utembee?' 6 Lakini mtambue ya kwamba
Mwana wa Adamu anao uwezo wa kusamehe dhambi...” aliyasema haya kwa yule
aliyepooza, “Simama, chukua godoro lako, na uende nyumbani kwako” 7 Ndipo yule
mtu akasimama na kuondoka kwenda nyumbani kwake. 8 Makutano walipoona
hayo, walishangaa na kumsifu Mungu, ambaye amewapa uwezo huo watu. 9 Na Yesu
alipokuwa akipita kutoka hapo, alimwona mtu ambaye aliitwa kwa jina la Mathayo,
ambaye alikuwa amekaa sehemu ya watoza ushuru. Naye akamwambia, “Nifuate
mimi” Naye akasimama na kumfuata. 10 Na Yesu alipoketi ili ale chakula ndani ya
nyumba, wakaja watoza ushuru wengi na watu waovu wakashiriki chakula pamoja
na Yesu na wanafunzi wake. 11 Ndipo Mafarisayo walipoona hayo, wakawaambia
wanafunzi “Kwa nini mwalimu wenu anakula chakula pamoja na watoza ushuru
na watu waovu?” 12 Yesu aliposikia hayo, naye alisema “ Watu walio na afya
nzuri hawahitaji mganga, isipokuwa wale walio wagonjwa. 13 Inawapasa muende
mkajifunze maana yake, “Ninapenda rehema na siyo dhabihu” Kwa kuwa nilikuja,
si kwa wenye haki kutubu, lakini kwa wenye dhambi. 14 Ndipo wanafunzi wa
Yohana wakaja kwake na kusema, “Kwa nini sisi na mafarisayo tunafunga, lakini
wanafunzi wako hawafungi?” 15 Yesu akawaambia, Je wasindikizaji wa arusi
wanaweza kuwa na huzuni pindi Bwana arusi anapokuwa pamoja nao? Lakini siku
zinakuja ambapo Bwana arusi atachukuliwa kutoka kwao, na ndipo watakapofunga.

16 Hakuna mtu anayeweka kipande cha nguo mpya kwenye nguo ya zamani, kiraka
kitatatuliwa kutoka kwenye nguo na mpasuko mkubwa utatokea. 17 Hakuna watu
wanaoweka mvinyo mpya katika chombo cha mvinyo wa zamani, ikiwa watafanya,
ngozi itachanika, mvinyo utatoweka na ngozi itaharibika. Badala yake, huweka
mvinyo mpya katika ngozi mpya na vyote vitakuwa salama. 18 Wakati Yesu
alipokuwa akiwaambia mambo hayo, tazama, afisa akaja akasujudu mbele yake,
Naye akasema, " Binti yangu amefariki punde, lakini njoo na uweke mkono wako
juu yake na yeye ataishi tena. 19 Ndipo Yesu akasimama na kumfuata na wanafunzi
wake pia. 20 Tazama, mwanamke ambaye alikuwa anatokwa damu kwa muda wa
miaka kumi na miwili, akaja karibu na Yesu na akagusa sehemu ya pindo la vazi
lake. 21 Kwa kuwa alisema, "Endapo nitagusa vazi lake, nami nitapata uponyaji."
22 Yesu akageuka na kumtazama na kumwambia. "Binti, jipe moyo, imani yako
imekufanya upone," Na muda huo huo mwanamke akapata uponyaji muda huo.
23 Na Yesu alipofika kwenye nyumba ya afisa, naye aliwaona wapiga tarumbeta
na umati wa watu ulikuwa ukipiga kelele. 24 Naye akasema, "Tokeni hapa, kwa
kuwa binti hajafa, bali amelala. Lakini wao walicheka na kumkebehi. 25 Na wale
watu walipotolewa nje, naye akaingia chumbani na kumshika mkono na msichana
akaamka. 26 Na habari hizi zikaenea katika mji mzima. 27 Ndipo Yesu alipokuwa
akipita kutoka pale, wanaume wawili vipofu wakamfuata. Waliendelea kupaza
sauti wakisema, "Tunaomba uturehemu, Mwana wa Daudi." 28 Pindi Yesu apokuwa
amefika kwenye nyumba, wale vipofu wakaja kwake. Yesu akawaambia, "Mnaamini
kwamba ninaweza kutenda?" Nao wakamwambia "Ndiyo, Bwana" 29 Ndipo Yesu
akagusa macho yao na kusema "Na ifanyike hivyo kwenu kama imani yenu ilivyo"
30 Na macho yao yakafumbuka. Ndipo Yesu akasisitiza akawaamuru na kusema
"Angalieni mtu yeyote asifahamu kuhusu jambo hili." 31 Lakini watu hawa wawili
wakaondoka na kutangaza habari hizi sehemu zote za mji. 32 Ndipo wale wanaume
wawili walipokuwa wakienda zao, Tazama, mtu mmoja bubu aliyepagawa na pepo
akaletwa kwa Yesu. 33 Na pepo walipomtoka, yule mtu bubu akaanza kuongea. Umati
ukashangazwa na kusema "Hii haijawahi kutokea katika Israel. 34 Lakini mafarisayo
walikuwa wakisema " Kwa wakuu wa pepo, anawafukuza mapepo" 35 Yesu akaenda
kwenye miji yote na vijiji. Naye akaendelea kufundisha katika masinagogi, akihubiri
injili ya ufalme, na kuponya magonjwa ya kila aina na udhaifu wa aina zote. 36 Wakati
alipotazama umati, naye aliwaonea huruma, kwa sababu walisumbuka na kuvunjika
moyo. Walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji. 37 Naye akawaambia wanafunzi
wake. "Mavuno ni mengi, lakini wafanya kazi ni wachache. 38 Hivyo basi upesi
mwombeni Bwana wa mavuno, ili kwamba atume wafanya kazi katika mavuno
yake."

# 10

1 Yesu akawaita wanafunzi wake kumi na wawili pamoja na kuwapa mamlaka
juu ya pepo wachafu, kuwakemea na kuwafukuza na kuponya aina zote za maladhi
na aina zote za magonjwa. 2 Majina ya mitume kumi na wawili ni haya. La
kwanza simeoni (ambaye pia anaitwa Petro), na Andrea kaka yake, Yakobo mwana
wa Zebedayo, na Yohana kaka yake: 3 Philipo, na Bartelemayo, Thomaso, na
Mathayo mtoza ushuru, Yakobo mwana wa Alfayo, na Tadeo, 4 Simoni mkananayo,
na Yuda iskariote, ambaye alimsaliti. 5 Hawa kumi na wawili Yesu aliwatuma.
Naye aliwaelekeza akisema "Msiende sehemu wanakoishi wamataifa na msiingie
kwenye miji ya wasamalia. 6 Badala yake, mwende kwa kondoo waliopotea wa
nyumba ya Israel. 7 Na mnapokwenda, hubirini na kusema, ufalme wa mbinguni
umekaribia.' 8 Ponyeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma na fukuzeni

pepo. Mmepokea bure, toeni bure. 9 Msichue dhahabu, almasi au shaba kwenye pochi
zenu. 10 Usichukue mkoba katika safari yenu, au nguo za ziada, viatu au fimbo, kwa
kuwa mfanyakazi anastahili chakula chake. 11 Mji wowote au kijiji mtakachoingia,
tafuteni ambaye anastahili na mkae pale mpaka mtakapoondoka. 12 Mtakapoingia
katika nyumba salimieni, 13 endapo nyumba inastahili, amani yenu ibaki pale,
lakini kama nyumba haistahili, amani yenu iondoke pamoja nanyi. 14 Na kwa wale
wasiowapokea ninyi au kusikiliza maneno yenu, wakati mnaondoka kwenye nyumba
au mji huo, jipanguseni mavumbi ya nyayo zenu mahali hapo. 15 Kweli ninawaambia,
itakuwa ya kustahimili zaidi miji ya Sodoma na Gomorah siku ya hukumu kuliko
mji huo. 16 Angalia, ninawatuma kama kondoo katikati ya mbwa mwitu, kwa hiyo
iweni na werevu kama nyoka na wapole kama njiwa. 17 Muwe waangalifu na
watu, watawapeleka kwenye mabaraza, na watawapiga kwenye masinagogi. 18 Na
mtaletwa mbele ya wakuu na wafalme kwa ajili yangu, kama ushuhuda kwao na
kwa mataifa. 19 Pindi watakapowashutumu, msiwe na wasiwasi jinsi gani au nini
cha kuongea, kwa kuwa kitu cha kusema mtapewa kwa wakati huo. 20 Kwa kuwa
sio ninyi mtakaoongea, lakini Roho wa Baba yenu ataongea ndani yenu. 21 Ndugu
atamwinukia ndugu yake kumwua, na baba kwa mtoto wake. Watoto watainuka
dhidi ya wazazi, na kuwasababishia kifo. 22 Nanyi mtachukiwa na kila mtu kwa
sababu ya jina langu. Lakini yeyote atakayevumilia mpaka mwisho mtu huyo
ataokolewa. 23 Pindi wanapowatesa katika mji huu, kimbilieni mji unaofuata, kwa
kweli ninawaambia, hamtakuwa mmekwenda kwenye miji yote ya Israeli kabla ya
mwana wa Adam hajarudi. 24 Mwanafunzi si mkuu kuliko mwalimu wake, wala
mtumwa aliye juu ya Bwana wake. 25 Inatosha kwa mwanafunzi kwamba awe
kama mwalimu wake, na mtumishi kama Bwana wake. Ikiwa wamemwita Bwana
wa nyumba Belzabuli, ni kwa kiasi gani zaidi watawakashifu wa nyumba yake!
26 Hivyo basi msiwahofu wao, kwa kuwa hakuna jambo ambalo halitafunuliwa, na
hakuna lililofichika ambalo halitajulikana. 27 Kile ninachowaambia gizani, mkiseme
nuruni, na mnachokisikia kwa ulaini masikioni mwenu, mkitangaze mkiwa juu ya
nyumba. 28 Msiwaogope wale ambao wanaua mwili lakini hawana uwezo wa kuua
roho. Badala yake, mwogopeni yule ambaye awezaye kuangamiza mwili na roho
kule kuzimu. 29 Je kasuku wawili hawauzwi kwa senti ndogo? Hata hivyo hakuna
anayeweza kuanguka chini bila Baba yenu kufahamu. 30 Lakini hata idadi ya nywele
zenu zimehesabiwa. 31 Msiwe na hofu, kwa kuwa mnathamani zaidi kuliko kasuku
wengi. 32 Hivyo basi kila mmoja atakaye nikiri mbele za watu, nami pia nitamkiri
mbele ya Baba yangu aliye mbinguni. 33 Lakini yeye atakaye nikana mbele za watu,
nami pia nitamkana mbele ya Baba yangu aliye mbinguni. 34 Msifikiri kwamba
nimekuja kuleta amani duniani. Sikuja kuleta amani, lakini upanga. 35 Kwa kuwa
nilikuja kumweka mtu apingane na baba yake, na binti dhidi ya mama yake, na mkwe
dhidi ya mama mkwe wake. 36 Adui wa mtu watakuwa wale wa nyumbani mwake.
37 Yeye ambaye anampenda baba au mama zaidi kuliko mimi huyo hanistahili.
Na yeye anayempenda kijana au binti zaidi kuliko mimi huyo hanistahili. 38 Yeye
ambaye hatabeba msalaba na kunifuata mimi hanistahili. 39 Yeye atakayetafuta
maisha atayapoteza. Lakini yeye atakayepoteza maisha kwa ajili yangu atayapata.
40 Yeye atakayewakaribisha amenikaribisha mimi, na yeye atakayenikaribisha mimi
amemkaribisha yeye aliyenituma mimi. 41 Na yeye atakayemkaribisha nabii kwa
sababu ni nabii atapokea thawabu ya nabii. Na yeye atakayemkaribisha mwenye
haki kwa sababu ni mtu wa haki atapokea thawabu ya mtu wa haki. 42 Yeyote
atakayempatia mmoja wa wadogo hawa, hata kikombe cha maji ya kunywa ya baridi,
kwa sababu yeye ni mwanafunzi, kweli ninawaambia, yeye hawezi kukosa kwa njia
yeyote thawabu yake."

# 11

1 Ikawa baada ya Yesu kumaliza kuwaelekeza wanafunzi wake kumi na wawili
aliondoka plae kwenda kufundisha na kuhubiri katika miji yao, 2 na Yohana akiwa
gereszani aliposikia akiwa juu ya matendo ya Kristo, alituma ujumbe kupitia
wanafunzi wake, 3 na wakamuuliza, “Wewe ni yule ajaye, au kuna mwingine
tunapaswa kumtazamia?” 4 Yesu akajibu na kusema kwao “Nendeni mkamtaarifu
Yohana yale mnayoyaona na yale mnayoyasikia. 5 Watu wasioona wanapata kuona,
viwete wanatembea, wakoma wanatakaswa, watu wasiosikia wanasikia tena, watu
waliokufa wanafufuliwa kupata uhai, na watu wahitaji wanahubiriwa habari njema.
6 Na amebarikiwa yule asiyeona shaka juu yangu. 7 Pindi watu hawa walipoondoka,
Yesu alianza kusema na umati juu ya Yohana, “Ni nini mlikwenda kuona katika
jangwa __tete likitikiswa na upepo? 8 Lakini nini mlikwenda kuona__mtu aliyevaa
mavazi mololo? Hakika, wale wavaao mavazi mololo hukaa katika nyumba za
wafalme. 9 Lakini mliondoka kuona nini-Nabii? Ndiyo, nawaambia, na zaidi ya
Nabii. 10 Huyu ndiye aliyeandikiwa, 'Tazama, namtuma mjumbe wangu mbele ya
uso wako, ambaye ataandaa njia yako mbele yako. 11 Mimi nawaambia kweli, kati ya
waliozaliwa na wanawake hakuna aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji. Lakini aliye
mdogo katika ufalme wa mbinguni ni mkubwa kuliko yeye. 12 Toka siku za Yohana
Mbatizaji mpaka sasa, ufalme wa Mbinguni ni wa nguvu, na watu wenye nguvu,
huuchukua kwa nguvu. 13 Kwa kuwa manabii na sheria, ikamelcuwa wakitabiri
mpaka kwa Yohana. 14 Na kamamko tayari kukubali, huyu ni Eliya, yule ajaye.
15 Aliye na masikio ya kusikia na asikie. 16 Nikilinganishe na nini kizazi hiki? Ni
mfano wa watoto wanaocheza maeneo ya sokoni, wanaokaa na kuitana 17 na kusema,
'Tuliwapigia zomari na hamkucheza. Tuliomboleza, na hamukulia.' 18 Kwa kuwa
Yohana alikuja bila kula mkate au kunywa mvinyo, na wakawa wanasema, 'Ana
pepo.' 19 Mwana wa Adamu alikuja akila na kunywa na wakasema 'Angalia, ni
mtu mlaji na mlevi, rafiki wa watoza ushuru na wenye dhambi!' Lakini hekima
inadhihirishwa kwa matendo yake.'' 20 Yesu alianza kuikemea miji ambamo baadhi
ya matendo yake ya ajabu yalitendeka, kwa sababu walikuwa hawajatubu, 21 Ole
wako, Kolazini, Ole wako Bethsaida! Kama matendo makuu yangetendeka Tiro na
Sidoni yale yaliyotendeka hapa, wangekuwa wametubu zamani kwa kuvaa magunia
na kujipaka majivu. 22 Lakini itakuwa uvumilivu kwa Tiro na Sidoni siku ya hukumu
kuliko kwako. 23 Wewe, Kapernaum, unadhani utainuliwa hadi mbinguni? Hapana
utashushwa hadi chini kuzimu. Kama kwa Sodoma kungefanyika matendo makuu,
kama yalifanyika kwako, ingekuwepo hadi leo. 24 Bali nasema kwako kwamba
itakuwa rahisi kwa nchi ya Sodoma kusimama siku ya hukumu kuliko wewe.
25 Katika muda huo Yesu alisema, “Nakusifu wewe, Baba, Bwana wa Mbingu na
Nchi, kwa sababu uliwaficha mambo haya wenye hekima na ufahamu, na kuyafunua
kwa wasio na elimu, kama watoto wadogo. 26 Baba kwa kuwa ilikupendeza hivyo
machoni pako. 27 Mambo yote yamekabidhiwa kwangu kutoka kwa Baba. Na hakuna
amjuaye Mwana isipokuwa Baba, na hakuna amjuaye Baba isipokuwa Mwana, na
yeyote ambaye Mwana ana hamu ya kumfunulia. 28 Njoni kwangu, nyinyi nyote
mnaosumbuka na mnaolemewa na mzigo mzito, nami nitawapumzisha. 29 Jitieni
nira yangu na mjifunze kutoka kwangu, kwa kuwa mimi ni mnyenyekevu na mpole
wa moyo na mtapata pumziko la nafsi zenu. 30 Kwa kuwa nira yangu ni laini na
mzigo wangu ni mwepesi.

# 12

1 Wakati huo Yesu aliendа siku ya sabato kupitia mashambani. Wanafunzi wake
walikuwa na njaa na wakaanza kuyavunja masuke na kuyala. 2 Lakini Mafarisayo

walipoona hayo, wakamwambia Yesu “Angalia wanafunzi wako wanavunja sheria
wanatenda siku yasiyo yuhusiwa siku ya Sabato'' 3 Lakini Yesu akawaambia,
“Hamjasoma jinsi Daudi aliyoyafanya, wakati alipokuwa na njaa, pamoja na watu
aliokuwa nao? 4 Namna alivyoingia ndani ya nyumba ya Mungu na kula mikate
ya wonyesho, ambayo ilikuwa siyo halali kwake kuila na wale aliokuwa nao, ila
halali kwa Makuhani? 5 Bado hamjasoma katika sheria, kwamba katika siku ya
Sabato Makuhani ndani ya hekalu huinajisi Sabato, lakini hawana hatia? 6 Lakini
nasema kwenu kuwa aliye mkuu kuliko hekalu yuko hapa. 7 Kama mngalijua hii
ina maanisha nini; nataka rehema na siyo dhabihu; msingaliwahukumu wasio na
hatia, 8 Kwa kuwa Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa Sabato.” 9 Kisha Yesu akatoka
pale akaenda katika sinagogi lao. 10 Tazama kulikuwa na mtu aliyepooza mkono.
Mafarisayo wakamuuliza Yesu, wakisema. “Je, ni halali kuponya siku ya Sabato?”
ili kwamba waweze kumshitaki kwa kutenda dhambi. 11 Yesu akawaambia, “Nani
kati yenu, ambaye ikiwa ana kondoo mmoja, na huyu kondoo akaanguka ndani ya
shimo siku ya sabato, hatamshika na kumtoa kwa nguvu ndani ya shimo? 12 Je, ni
kipi chenye thamani, zaidi kwani, si zaidi ya kondoo! Kwa hivyo ni halali kutenda
mema siku ya Sabato.'' 13 Kisha Yesu akamwambia yule mtu,” Nyoosha mkono
wako” Akaunyoosha, na ukapata afya, kama ule mwingine. 14 Lakini Mafarisayo
wakatoka njena wakapanga jinsi ya kumwangamiza walienda nje kupanga kinyume
chake. Walikuwa wakitafuta jinsi ya kumuua. 15 Yesu alipoelewa hili aliondoka hapo.
Watu wengi walimfuata, na akawaaponya wote. 16 Aliwaagiza wasije wakamfanya
afahamike kwa wengine, 17 kwamba itimie ile kweli, iliyokuwa imesemwa na nabii
Isaya, akisema, 18 Tazama, mtumishi wangu niliyemchagua, mpendwa wangu, katika
yeye nafsi yangu imependezwa. Nitaweka Roho yangu juu yake, na atatangaza
hukumu kwa Mataifa. 19 Hatahangaika wala kulia kwa nguvu; wala awaye yote
kusikia sauti yake mitaani. 20 Hatalivunja tete lililochubuliwa; hatazima utambi
wowote utoao moshi, mpaka atakapoleta hukumu ikashinda. 21 Na Mataifa watakuwa
na ujasiri katika jina lake. 22 Mtu fulani kipofu na bubu, aliyepagawa na pepo
aliletwa mbele ya Yesu. Akamponya, pamoja na matokeo ya kwamba mtu bubu
alisema na kuona. 23 Makutano wote walishangaa na kusema,”Yaweza mtu huyu
kuwa mwana wa Daudi?” 24 Lakini pindi Mafarisayo waliposikia muujiza huu,
walisema, “Huyu mtu hatoi pepo kwa nguvu zake mwenyewe isipokuwa kwa nguvu
za Belzebuli, mkuu wa pepo. 25 “Lakini Yesu alifahamu fikra zao na kuwaambia, “Kila
ufalme uliogawanyika wenyewe huharibika, na kila mji au nyumba inayogawanyika
yenyewe haitasimama. 26 Ikiwa Shetani, atamwondoa Shetani, basi anajipinga katika
nafsi yake mwenyewe. 27 Ni namna gani ufalme wake utasimama? Na kama natoa
pepo kwa nguvu za Belizabuli, wafuasi wenu huwatatoa kwa nija ya nani? Kwa
ajili ya hili watakuwa mahakimu wenu. 28 Na kama natoa pepo kwa nguvu za
Roho wa Mungu, basi ufalme wa Mungu umekjua kwenu. 29 Na mtu atawezaje
kuingia ndani ya nyumba ya mwenye nguvu na kuiba, bila kumfunga mwenye nguvu
kwanza? Ndiyo atakapoiba mali yake kutoka ndani ya nyumba. 30 Yeyote asiye
kuwa pamoja nami yuko kinyume changu, naye asiye kusanya pamoja nami huyo
hutawanya. 31 Kwa hiyo nasema kwenu, kila dhambi na kufuru watu watasamehewa,
ila kumkufuru Roho Mtakatifu hawatasamehewa. 32 Na yeyote asemaye neno
kinyume cha Mwana wa Adamu, hilo atasamehewa. Lakini yeyote asemaye kinyume
na Roho Mtakatifu, huyo hatasamehewa, katika ulimwengu huu, na wala ule ujao
33 Ama ufanye mti kuwa mzuri na tunda lake zuri, au uuharibu mti na tunda lake, kwa
kuwa mti hutambulika kwa tunda lake. 34 Nyinyi kizazi cha nyoka, nyie ni waovu,
mnawezaje kusema mambo mazuri? Kwa kuwa kinywa hunena kutoka katika akiba
ya yaliyomo moyoni. 35 Mtu mwema katika akiba njema ya moyo wake hutoka mema,

na mtu mwovu katika akiba ovu ya moyo wake, hutoa kilicho kiovu. 36 Nawaambia
kuwa katika siku ya hukumu watu watatoa hesabu ya kila neno lisilo na maana
walilosema. 37 Kwa kuwa kwa maneno yako utahesabiwa haki na kwa maneno
yako utahukumiwa.” 38 Kisha baadhi ya waandishi na Mafarisayo walimjibu Yesu
wakisema” Mwalimu, tungependa kuona ishara kutoka kwako.” 39 Lakini Yesu alijibu
na kuwaambia, “Kizazi kiovu na cha zinaa kinatafuta ishara. Lakini hakuna ishara
itakayotolewa kwao isipokuwa ile ishara ya Yona nabii. 40 Kama vile nabii Yona
alivyokuwa ndani ya tumbo la samaki mkubwa kwa siku tatu mchana na usiku,
hivyo ndivyo Mwana wa Adam atakavyo kuwa ndani ya moyo wa nchi kwa siku
tatu mchana na usiku. 41 Watu wa Ninawi watasimama mbele ya hukumu pamoja na
kizazi cha watu hawa na watakihukumu. Kwa kuwa walitubu kwa mahubiri ya Yona,
na tazama, mtu fulani mkuu kuliko Yona yuko hapa. 42 Malkia wa kusini atainuka
kwenye hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki na kukihukumu. Alikuja toka miisho
ya dunia kuja kusikia hekima ya Selemani, na tazama, mtu fulani mkuu kuliko
Selemani yupo hapa. 43 Wakati pepo mchafu amtokapo mtu, hupita mahali pasipo na
maji akitafuta kupumzika, lakini hapaoni 44 Kisha husema, 'nitarudi kwenye nyumba
yangu niliyotoka.' Arudipo hukuta ile nyumba imesafishwa na iko tayari. 45 Kisha
huenda na kuwaleta wengine roho wachafu saba walio wabaya zaidi kuliko yeye,
huja kuishi wote pale. Na hali yake ya mwisho huwa mbaya kuliko ya kwanza. Hivyo
ndivyo itakavyo kuwa kwa kizazi hiki kiovu. 46 Wakati Yesu alipokuwa akizungumza
na umati tazama, mama yake na ndugu zake walisimama nje, wakitafuta kuongea
naye. 47 Mtu mmoja akamwambia, “Tazama mama yako na ndugu zako wamesimama
nje, wanatafuta kuongea nawe”. 48 Lakini Yesu alijibu na kumwambia aliyemjulisha,
“Mama yangu ni nani? Na ndugu zangu ni akina nani?” 49 Naye alinyoosha mkono
wake kwa wanafunzi na kusema, “Tazama, hawa ni mama na ndugu zangu! 50 Kwa
kuwa yeyote afanyae mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni, mtu huyo ndiye ndugu
yangu, dada yangu na mama yangu”.

# 13

1 Katika siku hiyo Yesu aliondoka nyumbani na kukaa kando ya bahari. 2 Umati
mkubwa ulikusanyika kwa kumzunguka, aliingia ndani ya mtumbwi na kukaa ndani
yake. Umati wote walisimama kando ya bahari. 3 Kisha Yesu alisema maneno mengi
kwa mifano, Alisema, “Tazama, mpanzi alienda kupanda. 4 Alipokuwa akipanda
baadhi ya mbegu zilianguka kando ya njia na ndege walikuja wakazidonoa. 5 Mbegu
zingine zilianguka juu ya mwamba, ambapo hazikupata udongo wa kutosha. Ghafla
zilichipuka kwa sababu udongo haukuwa na kina. 6 Lakini jua lilipo chomoza
zilichomwa kwa sababu hazikuwa na mizizi, na zilikauka. 7 Mbengu zingine
zilianguka kati ya miti yenye miiba. Miti yenye miiba ilirefuka juu ikaisonga.
8 Mbegu zingine zilianguka kwenye udongo mzuri na kuzaa mbegu, zingine mara
mia moja zaidi, zingine sitini na zingine thelathini 9 Aliye na masikio na asikie.
10 Wanafunzi walikuja na kumwambia Yesu, “Kwa nini unazungumza na makutano
kwa mifano?” 11 Yesu alijibu kuwaambia, “Mmepewa upendeleo wa kufahamu
siri za ufalme wa mbinguni, bali kwao hawajapewa. 12 Lakini yeyote aliyenacho,
kwake yeye ataongezewa zaidi, na atapata faida kubwa. Ilasiye nacho hata kile
alichonacho atanyang'anywa. . 13 Hivyo naongea nao kwa mifano kwa sababu ingawa
wanaona, wasione kweli. Na ingawa wanasikia wasisikie wala kufahamu. 14 Unabii
wa Isaya umetimia kwao, ule usemao, “Msikiapo msikie, lakini kwa namna yoyote
hamtaelewa; wakati mwonapo muweze kuona, lakini kwa namna yeyote ile msijue.
15 Na mioyo ya watu hawa imekuwa giza, ni vigumu kusikia, na wamefumba macho
yao, ili wasiweze kuona kwa macho yao, au kusikia kwa masikio yao, au kufahamu

kwa mioyo yao, hivyo wangenigeukia tena, na ningewaponya.' 16 Bali macho yenu
yamebarikiwa, kwa kuwa yanaona, na masikio yenu kwa kuwa yanasikia. 17 Hakika
nawaambia manabii wengi na watu wenye haki walikuwa na hamu ya kuyaona
mambo yale myaonayo, na hawakuweza kuyaona. Walitamani kusikia mambo
yale mnayosikia, hawakuyasikia. 18 . Sasa sikilizeni mfano wa mpanzi. 19 Wakati
yeyote asikiapo neno la ufalme na asilifahamu, ndipo mwovu huja na kukinyakua
kilichokwisha kupandwa ndani ya moyo wake. Hii ni mbegu ile iliyopandwa kando
ya njia. 20 Yeye aliyepandwa katika miamba ni yule asikiaye neno na kulipokea
haraka kwa furaha. 21 Bado hana mizizi ndani yake, ila huvumilia kwa kitambo
kifupi. Wakati matatizo au mateso yanapotokea kwa sababu ya neno hujikwaa
ghafla. 22 Aliyepandwa kati ya miti ya miiba, huyu ni yule alisikiaye neno lakini
masumbuko ya ulimwengu na udaganyifu wa utajiri hulisonga lile neno lisije likazaa
matunda. 23 Aliyepandwa kwenye udongo mzuri, huyu ni yule asikiaye neno na
kulifahamu. Huyu ni yule azaaye matunda na kuendelea kuzaa moja zaidi ya mara
mia, nyingine sitini, nyingine thelathini.'' 24 Yesu aliwapa mfano mwingine. Akisema,
“Ufalme wa mbinguni unafananishwa na mtu aliye panda mbengu nzuri katika
shamba lake 25 Lakini watu waliposinzia, adui wake akaja pia akapanda magugu
katikati ya ngano kisha akaenda zake. 26 Baadaye ngano ilipoota na kutoa mazao
yake, ndipo magugu yalitokea pia. 27 Na watumishi wa mwenye shamba walikuja
wakamwambia, 'Bwana, hukupanda mbengu nzuri katika shamba lako? Imekuwaje
sasa lina magugu? 28 Akawaambia, Adui ametenda hili.' Watumishi walimwambia,
“Kwa hiyo unataka twende tukayang'oe?” 29 Mwenye shamba akisema, 'Hapana,
wakati mnayang'oa magugu mtang'oa pamoja na ngano. 30 Yaacheni yakue pamoja
mpaka wakati wa mavuno. Wakati wa mavuno nitasema kwa wavunaji, 'Kwanza
yang'oeri magugu na yafungeni matita matita na kuyachoma, lakini kusanyeni ngano
katika ghala langu.''' 31 Kisha Yesu aliwatolea mfano mwingine. Akasema, “Ufalme
wa mbinguni unafanana na mbegu ya haradali ambayo mtu aliichukua na kuipanda
katika shamba lake. 32 Mbegu hii kwa hakika ni ndogo kuliko mbegu zingine zote.
Lakini imeapo huwa kubwa kuliko mimea yote ya bustani, huwa mti, kiasi kwamba
ndege wa angani huja na kujenga viota katika matawi yake.” 33 Akawaambia mfano
mwingine tena.”Ufalme wa mbinguni ni kama chachu ile iliyo twaliwa na mwanamke
na kuichanganya kwa vipimo vitatu kwa unga mpaka viumuke. 34 Hayo yote
Yesu aliyasema kwenye umati kwa mifano. Na pasipo mifano hakusema chochote
kwao. 35 Hii ilikuwa kwamba kile kilichokwisha semwa kupitia kwa nabii kiweze
kutimia, pale aliposema, “Nitafumbua kinywa changu katika mifano. Nitasema
mambo yale yaliyokuwa yamefichwa tangu misingi ya ulimwengu”. 36 Kisha Yesu
aliwaacha makutano na kwenda nyumbani. Wanafunzi wake walimwendea na
kusema, “Tufafanulie mfano wa magugu ya shambani.'' 37 Yesu alijibu na kusema,
“Apandae mbegu nzuri ni Mwana wa Adamu. 38 Shamba ni ulimwengu; na mbegu
nzuri, hawa ni wana wa ufalme. Magugu ni wana wa yule mwovu, na adui aliye
zipanda ni ibilisi. 39 Na mavuno ni mwisho wa ulimwengu, na wavunaji ni malaika.
40 Kama vile magugu yanavyo kusanywa na kuchomwa moto, hivyo ndivyo itakavyo
kuwa mwisho wa ulimwengu. 41 Mwana wa Adamu atatuma malaika wake, na
kukusanya kutoka katika ufalme wake mambo yote yaliyosababisha dhambi na wale
watendao maasi. 42 Watawatupa wote katika tanuru la moto, ambako kutakuwa na
kilio na kusaga meno. 43 Ndipo watu wenye haki watakapong'aa kama jua katika
Ufalme wa Baba yao. Yeye aliye na masikio na sikie. 44 Ufalme wa mbinguni ni
kama hazina iliyofichwa shambani. Mtu akaiona na kuificha. Katika furaha yake
akaenda kuuza vyote alivyokuwa navyo, na kulinunua shamba. 45 Tena, ufalme
wa mbinguni ni kama mtu anayefanya biashara atafutaye lulu yenye thamani.

46 Wakati alipoiona ile yenye thamani, alienda akauza kila kitu alichokuwa nacho na
akainunua. 47 Ufalme wa mbinguni ni kama nyavu iliyo ndani ya bahari, na kwamba
hukusanya viumbe vya kila aina. 48 Ulipojaa wavuvi waliuvuta ufukweni. Kisha
wakakaa chini wakakusanya vitu vyema ndani ya vyombo, lakini visivyo na thamani
vilitupwa mbali. 49 Itakuwa namna hii katika mwisho wa dunia. Malaika watakuja
na kuwatenga watu waovu kutoka miongoni mwa wenye haki. 50 Na kuwatupa
ndani ya tanuru ya moto, ambako kutakuwa na maombolezo na kusaga meno.
51 Mmefahamu mambo yote haya? Wanafunzi walimjibu, ''Ndiyo.'' 52 Kisha Yesu
akawambia, ''Kila mwandishi ambaye amekuwa mwanafunzi wa ufalme anafanana
na mwenye nyumba atoaye katika hazina yake vitu vipya na vya kale.'' 53 IkawaYesu
alipomaliza mifano yote hiyo, akaondoka katika sehemu hiyo. 54 Kisha Yesu akafika
katika mkoa wake na akawafundisha watu katika sinagogi. Matokeo yake ni kuwa
walishangaa na kusema, “Ni wapi mtu huyu alipopata hekima hii na miujiza hii?
55 Mtu huyu siyo mwana wa seremala? Mariamu siyo mamaye? Na ndugu zake siyo
Yakobo, Yusuph, Simoni na Yuda? 56 Na dada zake tunao hapa petu? Basi mtu huyu
ameyapata wapi haya yote?”. 57 Aliwachukiza. Lakini Yesu aliwambia, “Nabii hakosi
kuwa na heshima isipokuwa kwao na katika nchi yao. 58 Na hakuweza kufanya
miujiza mingi kwa sababu hawakuwa na imani naye.

# 14

1 Kwa wakati huo, Herode alisikia habari juu ya Yesu.. 2 Akawaambia watumishi
wake, “Huyu ni Yohana Mbatizaji amefufuka kutoka katika wafu. Kwa hiyo nguvu
hizi zipo juu yake.” 3 Kwa kuwa Herode alikuwa amemkamata Yohana akamfunga
na kumtupa gerezani kwa sababu ya Herodia, mke wa Filipo kaka yake. 4 Kwa
kuwa Yohana alimwambia, “Si halali kumchukua yeye kuwa mke wake.” 5 Herode
angemwua lakini aliwaogopa watu kwa sababu walimwona Yohana kuwa nabii.
6 Lakini wakati siku ya kuzaliwa Herode ilipofika binti wa Herodia alicheza katikati
ya watu na kumpendeza Herode. 7 Katika kujibu kili aliahidi kwa kiapo kwamba
atampa chochote atakachoomba. 8 Baada ya kushauriwa na mama yake, alisema,
“Nipe mimi hapa katika kombe kichwa cha Yohana Mbatizaji.” 9 Mfalme alikuwa
na sikitiko kwa maombi ya binti, lakini kwa ajili ya kiapo chake, kwa sababu
ya wote waliokuwa chakulani pamoja naye aliamuru kwamba inapaswa ifanyike.
10 Alituma Yohana aletwe kutoka gerezani 11 ili akatwe kichwa chake na kikaletwa
juu ya sinia na akapewa binti na akakipeleka kwa mama yake. 12 Kisha wanafunzi
wake wakaja kuuchukua ule mwili na kuuzika, baada ya hili walienda kumwambia
Yesu. 13 Naye Yesu aliposika haya, akijatenga kutoka mahali pale akapanda ndani
ya mashuka akaenda sehemu iliyotengwa. Wakati umati ulipo fahamu alikokuwa,
walimfuata kwa miguu kutoka mijini. 14 Kisha Yesu alikuja mbele yao akauona
umati mkubwa. Akawaonea huruma na kuponya magonjwa yao. 15 Jioni ilipotimia,
wanafunzi wakaja kwake na kusema, “Hii ni sehemu ya jangwa, na siku tayari
imepita. Watawanyishe makutano ili waende vijijini wakanunue chakula kwa ajili
yao. 16 Lakini Yesu akawaambia, ''Hawana haja ya kwenda zao. Wapeni ninyi
chakula” 17 Wakamwambia, ''Hapa tunayo mikate mitano na samaki wawili tu.”''
18 Yesu akasema, “Ileteni kwangu.” 19 Kisha Yesu akauamuru umati kukaa chini ya
nyasi. Akachukuwa mikate mitano na samaki wawili. Akatazama juu mbinguni,
akabariki na kumega mikate akawapa wanafunzi. Wanafunzi wakaupatia umati.
20 Wakala wote na kushiba. Kisha wakavikusanya vipande vyote vya chakula na
kujaza vikapu kumi na mbili. 21 Wale waliokula walikadiriwa kuwa wanaume elfu
tano bila ya kusehabu wanawake na watoto. 22 Mara moja aliwaamuru wanafunzi
waingie ndani ya mashua, wakati huo yeye akawaaga umati waende zao. 23 Baada

ya kuwaaga umati kwenda zao, akapanda juu mlimani kuomba pekee yake. Wakati
ilipokuwa jioni alikuwa huko pekee yake. 24 Lakini sasa mashua ilipokuwa katikati ya
bahari ukiyumbayumba kwa sababu ya mawimbi, kwani upepo ulikuwa wa mpisho.
25 Katika usiku wa zamu ya nne Yesu aliwakaribia, akitembea juu ya maji. 26 Wakati
wanafunzi wake walipomwona akiitembea juu ya bahari, walihofu na kusema, “Ni
mzuka,'' na kupaaza sauti katika hali ya uoga. 27 Yesu akawaambia mara moja,
akisema, “Jipeni moyo! ni mimi! msiogope.” 28 Petro alimjibu kwa kusema, “Bwana,
kama ni wewe, niamuru nije kwako juu ya maji.'' 29 Yesu akasema, “Njoo.'' Hivyo
Petro akatoka ndani ya mashua na akatembea juu ya maji kwenda kwa Yesu. 30 Lakini
Petro alipoona mawimbi, aliogopa, na kuanza kuzama, chini, akaita sauti na kusema,
“Bwana, niokoe!'' 31 Haraka Yesu akanyoosha mkono wake akamnyanyua Petro, na
kumwambia, “Wewe mwenye imani ndogo, kwa nini ulikuwa na mashaka?” 32 Ndipo
Yesu na Petro walipoingia katika mashua, upepo ulikoma kuvuma. 33 Wanafunzi
mashuani wakamwabudu Yesu na kusema, “Kweli wewe ni Mwana wa Mungu.”
34 Na walipokwisha kuvuka, walifika katika nchi ya Genesareti. 35 Na watu katika
eneo lile walipomtambua Yesu, walituma ujumbe kila sehemu za kando, na kuleta
kila aliyekuwa mgonjwa. 36 Walimsihi kwamba waweze kugusha pindo la vazi lake,
na wengi walioligusa waliponywa.

# 15

1 Ndipo Mafarisayo na waadishi walikuja kwa Yesu kutoka Yerusalemu. Na kusema,
2 “Kwa nini wanafunzi wanayahalifu mapokeo ya wazee? Kwa kuwa hawanawi
mikono yao wanapokuwa wanakula chakula.'' 3 Yesu akawajibu na kuwaambia,
“Nanyi__kwa nini mnaihalifu sheria ya Bwana kwa ajili ya mapokeo yenu? 4 Kwa
kuwa Mungu alisema, 'Mheshimu baba yako na mama yako; na 'Asemaye uovu kwa
baba yake na mama yake, hakika atakufa.' 5 Lakini ninyi husema, 'Kila amwambiaye
baba yake na mama yake, '“Kila msaada ambao angepata kutoka kwangu sasa
ni zawadi kutoka kwa Mungu,''' 6 “Mtu huyo hana haja ya kumuheshimu baba
yake. Katika namna hii mmelitangua neno la Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu.
7 Enyi wanafiki, ni vema kama Isaya alivyo tabiri juu yenu aliposema, 8 'Watu
hawa wananiheshimu mimi kwa midomo yao, lakini mioyo yao iko mbali nami.
9 Wananiabudu bure, kwa sababu wanafundisha mafundisho yaliyo maagizo ya
wanadamu.”' 10 Ndipo akawaita makutano na kuwaambia,” Sikilizeni na mfahamu__
11 Hakuna kitu kiingiacho mdomoni mwa mtu na kumfanya najisi. Bali, kile
kitokacho kinywani, hiki ndicho kimfanyacho mtu kuwa najisi.'' 12 Ndipo wanafunzi
wakamwendea na kusema na Yesu, “Je!, Unafahamu Mafarisayo walipolisikia lile
neno walikwazika?” 13 Yesu aliwajibu na kusema, “Kila mmea ambao Baba yangu wa
mbinguni hajaupanda utang'olewa. 14 Waacheni pekee, wao ni viongozi vipofu. Kama
mtu kipofu atamuongoza kipofu mwenzake, wote wawili wataanguka shimoni.”
15 Petro akajibu na kumwambia Yesu,” Tuelezee mfano huu kwetu, 16 Yesu akajibu,
''Nanyi pia bado hamuelewi? 17 Ninyi hamuoni kuwa kila kiendacho mdomoni hupitia
tumboni na kwenda chooni?. 18 Lakini vitu vyote vitokavyo mdomoni hutoka ndani
ya moyo. Ndivyo vitu vimtiavyo mtu unajisi. 19 Kwa kuwa katika moyo hutoka
mawazo mabaya, uuaji, uzinzi, uasherati, wizi, ushuhuda wa uongo, na matusi.
20 Haya ndiyo mambo yamtiayo mtu unajisi. Lakini kula bila kunawa mikono
hakumfanyi mtu kuwa najisi.” 21 Ndipo Yesu akatoka mahali pale na akajitenga
kuelekea pande za miji ya Tiro na Sidoni. 22 Tazama akaja mwanamke Mkanani
kutoka pande hizo. Akapaza sauti akisema, ''Nihurumie, Bwana, Mwana wa Daudi;
binti yangu anateswa sana na pepo.'' 23 Lakini Yesu hakumjibu neno. Wanafunzi
wake wakaja wakimsihi, wakisema, ''Muondoe aende zake, maana anatupigia kelele.''

24 Yesu aliwajibu na kusema, Sikutumwa kwa mtu yeyoye isipokuwa kwa kondoo
waliopotea wa nyumba ya Israeli.'' 25 Lakini alikuja na kuinama mbele yake, akisema,
''Bwana nisaidie.'' 26 Alimjibu na kusema, “Siyo vema kuchukua chakula cha watoto
na kuwatupia mbwa,” 27 Akasema, “Ndiyo, Bwana, hata hivyo mbwa wadogo hula
chakula kiagukacho mezani mwa Bwana wao.” 28 Ndipo Yesu akajibu na akisema
“Mwanamke, imani yako ni kubwa. Na ifanyike kwako kama utakavyo.” Na binti
yake alikuwa ameponywa katika wakati huo. 29 Yesu aliondoka mahali pale na
kwenda karibu na bahari ya Galilaya. Kisha alienda juu ya mlima na kuketi huko.
30 Kundi kubwa likaja kwake. Na kumletea viwete, vipofu, bubu, vilema na wengine
wengi, waliokuwa wagonjwa. Waliwaweka katika miguu ya Yesu na akawaponya.
31 Nao umati wakashangaa walipoona mabubu wakiongea, na vilema wakifanywa
wazima, viwete wakitembea, na vipofu wakiona. Walimsifu Mungu wa Israeli. 32 Yesu
akawaita wanafunzi wake na kusema, “ Nimewaonea huruma umati, kwa sababu
wamekuwa nami kwa siku tatu bila kula kitu chochote. Sitawaaga waende kwao
bila kula, wasije wakazimia njiani.” 33 Wanafunzi wake wakamwambia, “Ni wapi
tunaweza kupata mikate ya kutosha hapa nyikani kushibisha umati mkuwbwa hivi?”
34 Yesu akawaambia, “Mna mikate mingapi?” Wakasema, “Saba, na samaki wadogo
wachache.” 35 Yesu akawaamuru umati uketi chini. 36 Aliitwaa ile mikate saba
na samaki, na baada ya kushukuru, akaimega na kuwapa wanafunzi. Wanafunzi
wakawapa umati. 37 Watu wote wakala na kutosheka. Na wakakusanya mabaki
ya vipande vya chakula vilivyosalia vipande vipande, vilijaa vikapu saba. 38 Wote
waliokula walikuwa wanaume elfu nne bila wanawake na watoto. 39 Kisha Yesu
akauaga umati waende zao na akaingia ndani ya mashua na kwenda sehemu za
Magadani.

# 16

1 Mafarisayo na Masadukayo walimjia na kumjaribu Yesu awaonyeshe ishara
inayotoka angani. 2 Lakini Yesu aliwajibu na kuwaambia kuwa “Ikiwa ni jioni
mnasema kuwa hali ya hewa ni nzuri, kwa kuwa anga ni jekundu. 3 Na asubuhi
mnasema 'Hali ya hewa leo si nzuri kwa kuwa anga ni jekundu na mawingu
yameifunika anga lote.' Mnajua kufasiri mwonekano wa anga, lakini hamwezi
kufasiri ishara za nyakati. 4 Kizazi kiovu na cha uzinzi kinatafuta ishara, lakini
hakuna ishara yoyote kitakachopewa, isipokuwa ile ya Yona. Kisha Yesu akawaacha
na akaenda zake. 5 Wanafunzi wakaja upande wa pili, lakini walikuwa wamesahau
kuchukua mikate. 6 Yesu akawaambia “ Jitahadharini na iweni makini na chachu ya
Mafarisayo na Masadukayo.” 7 Wanafunzi wakahojiana miongoni mwao na kusema.
“Ni kwa sababu hatukuchukua mikate.” 8 Yesu alitambua hilo na kusema, “Enyi
wenye imani ndogo, kwa nini mmewaza na kusemezana miongoni mwenu na kusema
kuwa ni kwa sababu hamkuchukua mikate? 9 Je bado hamtambui wala hamkumbuki
ile mikate mitano kwa watu elfu tano, na vikapu vingapi mlivyokusanya? 10 Au
mikate saba kwa watu elfu nne, na ni vikapu vingapi mlikuchukua? 11 Imekuwaje
kuwa hata hamuelewi ya kuwa nilikuwa sizungumzi nanyi juu ya mikate? Jitunzeni
na jihadharini na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo.” 12 Kisha wakatambua kuwa
alikuwa hawaambii juu ya kujihadhari na mikate iliyo na chachu, bali kujihadhari
na mafundisho ya Mafarisayo na Masadukayo. 13 Wakati Yesu alipofika sehemu za
Kaisaria ya Filipi, akawauliza wanafunzi wake, akisema, “Watu wanasema kuwa
Mwana wa Mtu ni nani?” 14 Wakasema,” Wengine husema kuwa ni Yohana Mbatizaji;
wengine, Eliya; na wengine, Yeremia, au mojawapo wa manabii. 15 Akawaambia,
ninyi mwasema mimi ni nani? 16 Kwa akijibu, Simoni Petro akasema, “Wewe ni
Kristo Mwana wa Mungu aliye hai” 17 Yesu akamjibu na kumwambia, “Umebarikiwa

wewe, Simoni Bar Yona, kwa kuwa damu na nyama havikukufunulia hili, bali Baba
yangu aliye mbinguni. 18 Nami pia ninakwambia kuwa wewe ni Petro, na juu ya
mwamba huu nitalijenga kanisa langu. Milango ya kuzimu haitalishinda. 19 Nitakupa
wewe funguo za ufalme wa mbinguni. Chochote utakachokifunga duniani kitakuwa
kimefungwa mbinguni, na chochote utakachokifungua duniani kitafunguliwa na
mbinguni.” 20 Kisha Yesu akawaamuru wanafunzi wasimwambie mtu yeyote kuwa
yeye alikuwa ni Kristo. 21 Tangu wakati huo Yesu alianza kuwaambia wanafunzi
kuwa ni lazima aende Yerusalemu, kuteswa kwa mambo mengi katika mikono ya
wazee na wakuu wa makuhani na waandishi, kuuawa na kufufuka siku ya tatu.
22 Kisha Petro akamchukua Yesu pembeni na kumkemea, kwa kusema, “Jambo
hili na liwe mbali nawe, Bwana, hili lisitokee kwako. 23 Lakini Yesu akageuka
na kumwambia Petro, “Rudi nyuma yangu shetani! Wewe ni kizuizi kwangu,
kwa maana hujali mambo ya Mungu, bali mambo ya wanadamu.” 24 Kisha Yesu
akawaambia wanafunzi wake, “Kama mtu yeyote akitaka kunifuata mimi, ni lazima
ajikane yeye mwenyewe, auchukue msalaba wake, na anifuate. 25 Kwa kuwa
anayetaka kuyaokoa maisha yake atayapoteza, na kwa yeyote anayepoteza maisha
yake kwa ajili yangu atayaokoa. 26 Je! Ni faida gani atakayopata mtu akipata
dunia yote lakini akapoteza maisha yake? Je! Ni kitu gani atakachotoa mtu katika
kubadilishana na maisha yake? 27 Kwa kuwa Mwana wa Adamu atakuja katika
utukufu wa Baba yake na malaika wake. Naye atamlipa kila mtu kulingana na
matendo yake. 28 Kweli nawaambieni kuna baadhi yenu mliosimama hapa ambao
hawataonja mauti mpaka watakapomwona Mwana wa Adamu akija katika ufalme
wake.

# 17

1 Siku sita baadaye Yesu aliwachukua pamoja naye Petro, na Yakobo, na Yohana
nduguye, na akawachukua mpaka juu ya mlima mrefu wao wenyewe. 2 Alibadilishwa
mbele yao. Uso wake ukang'aa kama jua, na nguo zake zilionekana zenye kung'aa
kama nuru. 3 Tazama, pale walitokea Musa na Eliya wakiongea naye. 4 Petro akajibu
na kumwambia Yesu, “Bwana, ni vema kwetu sisi kuwepo mahali hapa. Kama
ukitamani, nitajenga hapa vibanda vitatu - kimoja chako, na kimoja kwa ajili ya
Musa, na kimoja kwa ajili ya Eliya.” 5 Wakati anaongea, tazama wingu jeupe likawatia
kivuli, na tazama, ikatokea sauti toka kwenye wingu, ikisema, “Huyu ni Mwanangu
mpendwa ninayependezwa naye. Msikilizeni yeye.” 6 Wanafunzi waliposikia
hayo, wakaanguka kifudifudi na wakaogopa sana. 7 Kisha Yesu akaja akawagusa
na kusema, “Inukeni wala msiogope.” 8 Nao wakainua nyuso zao juu lakini
hawakumwona mtu isipokuwa Yesu pekee. 9 Na walipokuwa wakishuka mlimani,
Yesu akawaagiza, akasema, “Msitoe habari ya maono hayo mpaka Mwana wa Adamu
atakapofufuka kutoka katika wafu.” 10 Wanafunzi wake wakamwuliza, wakisema, “
Ni kwanini waandishi wanasema kuwa Eliya atakuja kwanza? 11 Yesu akawajibu na
kusema, “Eliya atakuja kweli na atarudisha mambo yote. 12 Lakini naawaambieni
ninyi, Eliya amekwisha kuja, lakini hawakumtambua. Badala yake, walimfanyia
mambo watakayo wao. Na hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyoteswa katika
mikono yao.” 13 Ndipo wanafunzi wakatambua kuwa alikuwa akiongea habari za
Yohana Mbatizaji. 14 Walipofika katika umati wa watu, mtu mmoja alimwendea,
akapiga magoti mbele zake, na kumwambia, 15 “Bwana, umhurumie mwanangu,
maana amekuwa na kifafa na kuteseka sana. Kwa kuwa mara nyingi huanguka
motoni au kwenye maji. 16 Nilimleta kwa wanafunzi wako, lakini hawakuweza
kumponya. 17 Yesu akajibu akisema, “Enyi Kizazi kisichoamini na kilichoharibika,
nitakaa pamoja nanyi mpaka lini? Nitavumiliana nanyi hata lini? Mlete hapa

kwangu.” 18 Yesu alimkemea, na pepo akamtoka. Kijana aliponywa tangu saa ile.
19 Kisha wanafunzi wakamjia Yesu kwa siri na kumwuliza, “Kwanini hatukuweza
kumfukuza?” 20 Yesu akawaambia, “Kwa sababu ya imani yenu ndogo. Kweli
nawaambieni, kama mtakuwa na imani hata ndogo kama punje ya mbegu ya
haradali, mtaweza kuuambia mlima huu, hama kutoka hapa uende kule, nao
utahama na hakutakuwa na kitu chochote cha kushindikana kwenu. 21 (Zingatia:
Maneno ya msitari wa 21 “Lakini, aina hii ya pepo haiwezekani kutoka, ila kwa
maombi na Kufunga” hayaonekani katika nakala bora za kale). 22 Wakati wakiwa
bado Galilaya, Yesu akawaambia Wanafunzi wake, “Mwana wa Adamu atatiwa
mikononi mwa watu. 23 Na watamwua, na siku ya tatu atafufuka.” Wanafunzi
walihuzunika sana. 24 Nao walipofika Kapenaumu, watu wakusanyao kodi ya nusu
shekeli wakamwendea Petro na kusema, “Je mwalimu wenu hulipa kodi ya nusu
shekeli?” 25 Akasema, “Ndiyo” Lakini Petro alipoingia ndani ya nyumba, Yesu
akaongea na Petro kwanza na kusema, “ Unafikiria nini Simon? Wafalme wa
dunia, hupokea kodi au ushuru kutoka nani? Kwa wale wanaowatawa kutoka kwa
wageni? 26 Na wakati Petro aliposema, “Kutoka kwa wageni” Yesu akamwambia,
hivyo watawaliwa wameondolewa katika ulipaji. 27 Lakini tusije tukawafanya watoza
ushuru wakatenda dhambi, nenda baharini, tupa ndoano, na umtwae yule samaki
ajaye kwanza. Baada ya kuufungua mdomo wake, utakuta mle shekeli moja. Ichukue
na uwape watoza ushuru kwa ajili yangu na wewe.

## 18

1 Muda huo huo wanafunzi wakaja kwa Yesu na kumwambia, “Ni nani aliye
mkubwa katika ufalme wa mbinguni?” 2 Yesu akamwita mtoto mdogo, akamweka
katikati yao, 3 na kusema, “Kweli nawaambieni, msipotubu na kuwa kama watoto
wadogo hamtaweza kuingia katika ufalme wa Mungu. 4 Hivyo yeyote ajishushaye
kama mtoto mdogo, mtu kama huyo ni mkuu katika ufalme wa mbinguni. 5 Na
yeyote ampokeaye mtoto mdogo kwa jina langu anipokea mimi. 6 Lakini yeyote
asababishaye mmoja kati ya wadogo hawa wanaoniamini kuasi, itakuwa vizuri kwa
mtu huyo jiwe kuu la kusagia likafungwa shingoni mwake, na kuzamishwa kilindini
mwa bahari. 7 Ole kwa dunia kwa sababu ya wakati wa kukwazwa! kwa kuwa haina
budi kwa nyakati hizo kuja, lakini ole kwake kwa mtu yule nyakati hizo zitakuja kwa
ajili yake! 8 kama mkono wako au mguu wako ukikusababishia kukwazika, ukate na
uutupe mbali na wewe. Ni vizuri zaidi kwako wewe kuingia kwenye uzima ukiwa
bila mkono au kilema, kuliko kutupwa kwenye moto wa milele ukiwa na mikono yote
au miguu yote. 9 Kama jicho lako likikukwaza, uling`oe na ulitupe mbali na wewe. Ni
vizuri zaidi kwako wewe uingie kwenye uzima na jicho moja, kuliko kutupwa kwenye
moto wa milele ukiwa na macho yote. 10 Tazameni kwamba msije mkamdharau
mmoja wa wadogo hawa. Kwa maana nawambieni kuwa mbinguni kuna malaika
wao siku zote wakiutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni. 11 (Zingatia: Maneno
yanayoonekana kama ya msitari wa 11, “Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kuokoa
kile kilichokuwa kimepotea” hayakuonekana katika nakala bora za kale). 12 Mnafikiri
nini? Ikiwa mtu ana kondoo mia moja, na mmoja wao akapotea, je hatawaacha tisini
na tisa ya mlimani na kwenda kumtafuta mmoja aliyepotea? 13 Na akiisha kumpata,
kweli nawaambieni, anamfurahia kuliko wale tisini na tisa wasiopotea. 14 Vivyo
hivyo, siyo mapenzi ya Baba yenu wa mbinguni kuwa mmoja wa wadogo hawa
aangamie. 15 Kama ndugu yako akikukosea, nenda, kamwonyeshe dosari iliyopo kati
yako na yeye akiwa pekee yake. Kama akikusikiliza, utakuwa umemrejesha ndugu
yako. 16 Lakini kama hatakusikiliza, mchukue ndugu mmoja au wawili zaidi pamoja
nawe, kwa kuwa kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno linaweza

kuthibitishwa. [17] Na kama akipuuza kuwasikiliza, liambie kanisa jambo hilo, kama
akipuuza vilevile kulisikiliza kanisa, basi na awe kama mtu wa mataifa na mtoza
ushuru. [18] Kweli nawaambieni, chochote kile mtakachokifunga duniani na mbinguni
kitafungwa. na chochote mtakachokifungua duniani na mbinguni kitafunguliwa.
[19] Tena nawaambieni kwamba kama watu wawili kati yenu wakikubaliana juu ya
jambo lolote duniani waliombalo, hilo Baba yangu wa mbinguni atalifanya. [20] Kwa
kuwa wawili au watatu wakikusanyika pamoja kwa jina langu, Mimi niko katikati
yao. [21] Tena Petro akaja na kumwambia Yesu, “Bwana, ni mara ngapi ndugu yangu
akinikosea nami nimsamehe? Hata mara saba?” [22] Yesu akamwambia, “Sikuambii
mara saba, lakini hata sabini mara saba. [23] Kwa sababu hiyo ufalme wa mbinguni
ni sawa na mfalme fulani aliyetaka kusahihisha hesabu kutoka kwa watumwa wake.
[24] Alipoanza kusahihisha hesabu, mtumwa moja akaletwa kwake ambaye alikuwa
anamdai talanta elfu kumi. [25] Kwa kuwa hakuwa na njia ya kulipa, bwana wake
aliagiza auzwe, mke wake pamoja na watoto wake na kila kitu alichokuwa nacho,
na malipo yafanyike. [26] Hivyo mtumwa alianguka, akapiga magoti mbele yake,
akisema, 'Bwana, uwe na uvumilivu pamoja nami, na nitakulipa kila kitu.' [27] Hivyo
bwana wa yule mtumwa, kwa kuwa alisukumwa sana na huruma, alimwachilia na
kumsamehe deni hilo [28] Lakini mtumwa yule alitoka na kumpata mmoja kati ya
watumwa wenzake, aliyekuwa anamdai denari mia. Alimvuta, akamkaba kooni, na
kumwambia, 'Nilipe kile ninachokudai.' [29] Lakini yule mtumwa mwenzake alianguka
na kumsihi sana, akisema, 'Uwe na uvumilivu nami, na nitakulipa.' [30] Lakini
mtumwa yule wa kwanza alikataa. Badala yake, aliendа na kumtupa gerezani,
mpaka atakapo mlipa kile anachomdai. [31] Na walipoona watumwa wenzake kile
kilichotokea. Walisikitishwa sana. Walikuja na kumwambia bwana wao kila kitu
kilichotokea. [32] Ndipo yule bwana wa mtumwa yule alimwita, na kumwambia,
'Ewe mtumwa mwovu, nilikusamehe wewe deni langu lote kwa sababu ulinisihi
sana. [33] Je! Haukutakiwa kuwa na huruma kwa mtumwa mwenzio, kama mimi
nilivyokuhurumia wewe? [34] Bwana wake alikasirika na kumkabidhi kwa wale
watesaji mpaka atakapolipa kiasi chote alichokuwa anadaiwa. [35] Hivyo ndivyo Baba
yangu wa Mbinguni atakavyowafanyia, kama kila mmoja wenu hatamsamehe ndugu
yake kutoka moyoni mwenu.”

# 19

[1] Ilitokea wakati Yesu alipomaliza maneno hayo, akaondoka Galilaya, na akaenda
mpakani mwa Yudea mbele ya mto Jordani. [2] Umati mkubwa ukamfuata, na
akawaponya huko. [3] Mafarisayo wakamjia, wakamjaribu, wakamwambia, “Je ni
halali kwa mtu kumwacha mke wake kwa sababu yoyote?” [4] Yesu akajibu na
kusema, “Hamkusoma, kwamba yeye aliyewaumba mwanzo aliwaumba mume na
mke? [5] Na tena akasema, 'Kwa sababu hiyo mwanaume atamwacha baba yake
na mama yake na kuungana na mke wake, nao wawili watakuwa mwili mmoja?'
[6] Hivyo siyo wawili tena, bali mwili mmoja. Basi, kile alichokiunganisha Mungu,
mtu yeyote asikitenganishe.” [7] Wakamwambia, “Sasa kwa nini Musa alituamuru
kutoa hati ya talaka na kumwacha?” [8] Akawaambia, “Kwa ugumu wenu wa mioyo
Musa aliwaruhusu kuwaacha wake zenu, lakini tangu mwanzo haikuwa hivyo.
[9] Nawaambieni, kwamba yeyote atayemwacha mke wake, isipokuwa kwa sababu
ya uzinzi, na akamwoa mwingine, amezini. Na mwanaume atakayemwoa mke
aliyeachwa amezini.” [10] Wanafunzi wakamwambia Yesu, “Kama ndivyo ilivyo kwa
mume na mkewe, siyo vizuri kuoa.” [11] Lakini Yesu akawaambia, “Si kila mtu
anaweza kupokea mafundisho haya, bali ni kwa wale tu walioruhusiwa kupokea.
[12] Kwa vile wapo matowashi waliozaliwa tokea tumboni mwa mama zao. Na

vilevile kuna matowashi waliofanywa na watu. Na kuna matowashi waliojifanya
matowashi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Awezaye kupokea mafundisho haya
na ayapokee." [13] Kisha akaletewa baadhi ya watoto wadogo ili awawekee mikono
juu yao na kuomba, lakini wanafunzi wake wakawakemea. [14] Bali Yesu akasema,
"Waruhusuni watoto wadogo, wala msiwakataze kuja kwangu, kwa maana ufalme
wa mbinguni ni wa watu kama wao. [15] Naye akaweka mikono yake juu yao, na
kisha akaondoka pale. [16] Tazama mtu mmoja akaja kwa Yesu na kusema, "Mwalimu,
ni kitu gani kizuri ninachotakiwa kufanya ili nipate kuwa na uzima wa milele?"
[17] Yesu akamwambia, "Kwa nini unaniuliza ni kitu gani kizuri? Kuna mmoja tu aliye
mwema, lakini kama ukitaka kupata uzima, shika sheria za Mungu." [18] Yule mtu
akamwuliza, "Ni sheria zipi?" Yesu akasema, "Usiue, usizini, usiibe, usishuhudie
uongo, [19] waheshimu baba yako na mama yako, na mpende jirani yako kama nafsi
yako." [20] Mtu yule akamwambia, "Mambo yote hayo nimeyatii. Bado ninahitaji
nini? [21] "Yesu akamwambia, "Kama ukitaka kuwa mkamilifu, nenda, ukauze ulivyo
navyo, na uwape maskini, na utakuwa na hazina mbinguni. Kisha njoo unifuate."
[22] Lakini kijana yule aliposikia yale Yesu aliyomwambia, akaondoka kwa huzuni, kwa
sababu alikuwa na amemiliki mali nyingi. [23] Yesu akawaambia wanafunzi wake,
"Kweli nawaambieni, ni vigumu kwa mtu tajiri kuingia katika ufalme wa mbinguni.
[24] Tena nawaambieni, ni rahisi kwa ngamia kupita katika tundu la sindano, kuliko
kwa mtu tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu." [25] Wanafunzi waliposikia hivyo,
wakashangaa sana na kusema, "Ni yupi basi atakayeokoka?" [26] Yesu akawatazama na
kusema, "Kwa wanadamu hilo haliwezekani, lakini kwa Mungu yote yanawezekana."
[27] Kisha Petro akamjibu na kumwambia, "Tazama, tumeacha vyote na kukufuata
wewe. Ni kitu gani tutakachopata?" [28] Yesu akawaambia, "Kweli nawaambieni,
yeye aliyenifuata mimi, katika uzao mpya wakati Mwana wa Adam atakapoketi
katika kiti cha enzi cha utukufu wake, ninyi pia mtaketi juu ya viti kumi na viwili
vya enzi, kuwahukumu makabila kumi na mawili ya Israeli. [29] Kila mmoja wenu
aliyeacha nyumba, kaka, dada, baba, mama, watoto, au shamba kwa ajili ya jina
langu, atapokea mara mia na kuurithi uzima wa milele. [30] Lakini wengi walio wa
kwanza sasa, watakuwa wa mwisho, na walio wa mwisho watakuwa wa kwanza.

# 20

[1] Kwa maana ufalme wa mbinguni unafanana na mmliki wa shamba, aliyeamka
asubuhi na mapema ili kuajiri wafanyakazi katika shamba lake la mizabibu. [2] Baada
ya kuwa amekubaliana na wafanyakazi dinari moja kwa kutwa, aliwatuma kwenda
katika shamba lake la mizabibu. [3] Alienda tena baada ya masaa matatu hivi na
aliona wafanyakazi wengine wakiwa wamesimama bila kazi katika eneo la soko.
[4] Akawaambia, 'Ninyi pia, nendeni katika shamba la mizabibu, na chochote kilicho
halali nitawapa.' Hivyo wakaenda kufanya kazi. [5] Akaenda tena baada ya masaa
sita na tena katika saa ya tisa, na alifanya hivyo hivyo. [6] Mara nyingine tena
mnamo saa kumi na moja, alienda na kuwakuta watu wengine wamesimama bila
kazi. Aliwaambia, 'kwanini mmesimama hapa bila kazi yoyote kwa siku nzima?
[7] Wakamwambia, kwasababu hakuna mtu yeyote aliyetuajiri. Akawaambia, 'Nanyi
ninyi pia nendeni katika shamba la mizabibu.' [8] Wakati wa jioni ulipofika, mwenye
shamba la mizabibu alimwambia msimamizi wake, 'Waite wafanyakazi na uwalipe
mishahara, kwa kuanza na wa mwisho hadi wa kwanza.' [9] Walipokuja wale
walioajiriwa saa kumi na moja, kila mmoja wao alipokea dinari. [10] Walipokuja
wafanyakazi wa kwanza, walifikiri kuwa watapokea zaidi, lakini walipokea pia kila
mmoja dinari moja kila mtu. [11] Baada ya kupokea malipo yao, walimlalamikia
mmiliki wa shamba. [12] Wakasema, 'Hawa wafanyakazi wa mwisho wametumia saa

moja tu katika kufanya kazi, lakini umewalinganisha na sisi, sisi tumebeba mzigo
kwa siku nzima na kuungua na joto.' 13 Lakini mwenye shamba akajibu na kusema
kwa mmoja wao, 'Rafiki, sikutenda jambo baya. Je! hatukukubaliana na mimi kwa
dinari moja? 14 Pokea kile kilicho halali yako na uende zako. Ni furaha yangu
kuwapa hawa wafanyakazi walioajiriwa mwisho sawa sawa na wewe. 15 Je! Si haki
kwangu kufanya kile ninachotaka na mali zangu? Au jicho lako ni ovu kwa sababu
mimi ni mwema? 16 Hivyo wa mwisho atakuwa kwanza na wa kwanza wa mwisho''
17 Yesu alipokuwa akipanda kwenda Yerusalem, aliwachukuwa wanafunzi wake kumi
na mbili pembeni, na njiani akawaambia, 18 ''Tazama tunaelekea Yerusalemu, na
Mwana wa Adamu atatiwa katika mikono ya wakuu wa makuhani na waandishi.
Watamhukumu kifo 19 na watamtoa kwa watu wa mataifa ili kumdhihaki, kumchapa
na kumsulibisha. Lakini katika siku ya tatu atafufuka.'' 20 Kisha mama wa wana
wa Zebedayo alikuja kwa Yesu na wana wake. Alipiga magoti mbele yake na
kumwomba kitu kutoka kwake. 21 Yesu akamwambia, “Unataka nini?” Akamwambia,
''Amuru kuwa hawa wanangu wawili wakae, mmoja mkono wako wa kulia na mmoja
mkono wako wa kushoto katika ufalme wako.'' 22 Lakini Yesu akajibu na kusema,
“Haujui kile unachoomba. Je! Unaweza kukinywea kikombe ambacho nitakinywea?”
wakamwambia, “Tunaweza.” 23 Akawaambia, “Kikombe changu hakika mtakinywea.
Lakini kukaa mkono wangu wa kulia na mkono wangu wa kushoto si jukumu
langu kuwapa, lakini ni kwa wale ambao wamekwisha kuandaliwa na Baba yangu.”
24 Wanafunzi wengine kumi waliposikia hivyo, wakahuzunishwa sana na wale ndugu
wawili. 25 Lakini Yesu aliwaita mwenyewe na kuwaambia, “Mnafahamu ya kuwa
watawala wa mataifa huwatiisha, na wakuu wao hutekeleza mamlaka juu yao.
26 Lakini isiwe hivyo kwenu. Badala yake, yeyote atakayetaka kuwa mkubwa
miongoni mwenu lazima awe mtumishi wenu. 27 Na atakaye kuwa wa kwanza
miongoni mwenu lazima awe mtumishi wenu. 28 Kama vile Mwana wa Adamu
hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa uhai wake kuwa ukombozi kwa wengi.”
29 Wakati wakitoka Yeriko, umati mkubwa ulimfuata. 30 Na waliwaona vipofu wawili
wameketi kando ya barabara. Waliposikia kuwa Yesu alikuwa anapita, walipaza sauti
na kusema, “Bwana, Mwana wa Daudi, utuhurumie.” 31 Lakini umati ukawakemea,
na kuwaambia nyamazeni. Hata hivyo, wao wakapaza sauti zaidi na kusema,
“Bwana, Mwana wa Daudi, utuhurumie.” 32 Kisha Yesu alisimama na aliwaita na
kuwauliza, “Mnataka niwafanyie nini?” 33 Wakamwambia, “Bwana kwamba macho
yetu yafumbuliwe.” 34 Basi Yesu, akiwa amevutwa na huruma, akayagusa macho yao,
mara hiyo, wakapokea uwezo wa kuona na wakamfuata.

# 21

1 Yesu na wanafunzi wake wakafika karibu na Jerusalemu na wakaenda mpaka
Bethfage, katika mlima mizeituni, kisha Yesu akawatuma wanafunzi wawili,
2 akiwaambia, “Nendeni katika kijiji kinachofuata, na mara moja mtamkuta punda
amefungwa pale, na mwanapunda pamoja naye. wafungueni na kuwaleta kwangu.
3 Ikiwa mtu yeyote akiwaambia chochote kuhusu hilo, mtasema, `Bwana anawahitaji,
` na mtu huyo mara moja atawaruhusu mje pamoja nao” 4 Jambo hili lilitokea
ni lile lililosemwa kupitia kwa nabii lazima litimizwe. Akawaambia, 5 Waambie
binti Sayuni, tazama, mfalme wako anakuja kwenu, mnyenyekevu na akiwa
amempanda punda, na mwana punda mme, mwana punda mchanga. 6 Kisha
wanafunzi waliondoka na kufanya kama Yesu alivyowaagiza. 7 Wakamleta punda
na mwanapunda, na kuweka nguo zao juu yao, naye Yesu akakaa pale. 8 Wengi
katika mkusanyiko walitandaza nguo zao njiani, na wengine walikata matawi
kutoka kwenye miti na kutandaza barabarani. 9 Umati uliomtangulia Yesu na

wale waliomfuata walipaza sauti, wakisema,"Hosana kwa mwana wa Daudi! Ni
mbarikiwa ajaye kwa jina la Bwana. Hosana juu zaidi!" 10 Yesu alipofika Yerusalemu,
mji mzima ulishtuka na kusema, "Huyu ni nani? 11 "Umati ulijibu, "Huyu ni Yesu
Nabii, kutoka Nazareti ya Galilaya." 12 Kisha Yesu akaingia katika hekalu la Mungu.
akawafukuza nje wote waliokuwa wakinunua na kuuza hekaluni. Pia alipindua meza
za wabadilishaji wa fedha na viti vya wauza njiwa. 13 Akawaambia, "Imeandikwa,
`'Nyumba yangu itaitwa nyumba ya maombi, `lakini ninyi mmeifanya pango la
wanyang`anyi." 14 kisha vipofu na vilema wakamjia hekaluni, naye akawaponya.
15 Lakini wakati wakuu wa makuhani na waandishi walipoona maajabu aliyoyatenda,
na waliposikia watoto wakipiga kelele hekaluni na kusema, "Hosana kwa Mwana
wa Daudi," walishikwa na hasira. 16 Wakamwambia, "Umesikia kile kinachosemwa
na hawa watu?" Yesu akawaambia, "Ndiyo! Lakini hamjawahi kusoma, 'Kutoka
kwa midomo ya watoto na watoto wachanga wanyonyao mna sifa kamili?'' 17 Kisha
Yesu akawaacha na kwenda nje ya mji katika Bethania na kulala huko. 18 Asubuhi
alipokuwa anarudi mjini, alikuwa na njaa. 19 Aliona mtini kandokando ya barabara.
Akauendea, lakini hakupata kitu juu yake isipokuwa majani. Aliuambia, "Kusiwe
na matunda kwako daima tena." Na mara hiyo mtini ule ukanyauka. 20 Wanafunzi
walipoona, wakastaajabu na kusema, "Imekuwaje mtini umenyauka mara moja?"
21 Yesu akajibu na kuwaambia, "Kweli nawaambieni, kama mkiwa na imani na
bila wasiwasi, hamtafanya kile kilichofanyika kwa huo mtini tu, lakini mtauambia
hata huo mlima, ` uchukuliwe na ukatupwe baharini, `na itafanyika. 22 Chochote
mtakachoomba kwa sala, huku mkiamini, mtapokea." 23 Yesu alipofika hekaluni,
wakuu wa makuhani na wazee wa watu wakamjia wakati alipokuwa akifundisha na
kumwuliza, "Ni kwa mamlaka gani unafanya mambo haya? Na ni nani aliyekupa
mamlaka haya?" 24 Yesu akajibu na kuwaambia, "Nami tena nitawauliza swali
moja. kama mkiniambia, nami vilevile nitawaambia ni kwa mamlaka gani ninafanya
mambo haya. 25 Ubatizo wa Yohana- ulitoka wapi, mbinguni au kwa wanadamu?"
Wakahojiana wenyewe, wakisema, tukisema, ulitoka mbinguni, `atatuambia, kwa
nini hamkumwamini? ` 26 Lakini tukisema, `ulitoka kwa wanadamu, `tunawaogopa
makutano, kwa sababu wote wanamwona Yohana kama nabii." 27 Kisha wakamjibu
Yesu na kusema, "Hatujui" Akawaambia pia, "Wala mimi sitawaambia ni kwa
mamlaka gani nafanya mambo haya. 28 Lakini mnafikiri nini? Mtu mwenye
wana wawili. Akaenda kwa moja na kumwambia, `Mwanangu, nenda ukafanye
kazi katika shamba la mizabibu 29 leo. `Mwana akajibu na kusema, `sitakwenda,
' Lakini baadaye akabadilisha mawazo yake na akaenda. 30 Na Mtu yule akaenda
kwa mwana wa pili na kusema kitu kilekile. Mwana huyu akajibu na kusema,
`nitakwenda, bwana', lakini hakwenda. 31 Yupi kati ya wana wawili aliyefanya
matakwa ya baba yake? Wakasema, "Mwana wa kwanza." Yesu akawaambia, "Kweli
nawaambieni, wakusanya ushuru na makahaba wataingia kwenye ufalme wa Mungu
kabla yenu kuingia. 32 Kwa maana Yohana alikuja kwenu kwa njia iliyo nyoofu,
lakini hamkumwamini, wakati wakusanya ushuru na makahaba walimwamini.
Na ninyi, mlipoona hilo likitendeka, hamkuweza kutubu ili baadaye mumwamini.
33 Sikilizeni mfano mwingine. Kulikuwa na mtu, mtu mwenye eneo kubwa la
ardh. Alipanda mizabibu, akaiwekea uzio, akatengeneza na chombo cha kukamlia
divai, akajenga na mnara wa walinzi, na akalikodisha kwa watunza zabibu. Kisha
akaenda katika nchi nyingine. 34 Wakati wa mavuno ya mizabibu ulipokaribia,
aliwatuma baadhi ya watumishi kwa wakulima wa mizabibu kuchukua mizabibu
yake. 35 Lakini wakulima wa zabibu wakawachukua watumishi wake, wakampiga
mmoja, wakamwua mwingine, na wakampiga mmoja kwa mawe. 36 Kwa mara
nyingine, Mmiliki aliwatuma watumishi wengine, wengi zaidi ya wale wa kwanza,

lakini wakulima wa mizabibu waliwatendea vilevile. 37 Baada ya hapo bwana yule
akamtuma kwao mwana wake, akisema, `'Watamheshimu mwanangu.'` 38 Lakini
wakulima wa mizabibu walipomwona kijana yule, wakaambizana, `'Huyu ni mrithi,
Njooni, tumuue na tumiliki urithi.' 39 `Hivyo wakamchukua, wakamtupa nje ya
shamba la mizabibu na kumwua. 40 Je mmliki wa shamba la mizabibu atakapokuja,
atawafanya nini wakulima wa mizabibu?" 41 Wakamwambia, "Atawaharibu hao
watu waovu katika njia ya ukali zaidi, na kisha atalikodisha shamba la mizabibu
kwa wakulima wengine wa mizabibu, watu ambao watalipa kwa ajili ya mizabibu
itakapoiva." 42 Yesu akawaambia, "Hamkusoma katika maandiko, 'Jiwe walilolikataa
waashi limekuwa jiwe kuu la msingi. Hili lilitoka kwa Bwana, na inashangaza
machoni petu?' 43 Hivyo nawaambieni, Ufalme wa Mungu utatwaliwa kutoka
kwenu na kupewa taifa linalojali matunda yake. 44 Yeyote atakayeanguka juu
ya jiwe hilo atavunjwa vipandevipande. Lakini kwa yeyote litakayemwangukia,
litamsaga." 45 Wakuu wa makuhani na mafarisayo waliposikia mifano yake, wakaona
kuwa anawazungumzia wao. 46 Lakini kila walipotaka kunyosha mikono juu yake,
waliogopa makutano, kwa sababu watu walimtazama kama nabii.

# 22

1 Yesu alisema nao tena katika mifano, akisema, 2 "Ufalme wa mbinguni unafanana
na mfalme aliyeandaa sherehe ya harusi ya mwanawe. 3 Akawatuma watumishi
wake kuwakaribisha waliokuwa wamealikwa kuja katika sherehe ya harusi, lakini
hawakufika. 4 Mfalme aliwatuma tena watumishi wengine, akisema. "Waambieni
wote walioalikwa, Angalieni, nimeandaa chakula. Fahali na ndama wangu wanono
wamechinjwa, na mambo yote yako tayari, Njoni katika sherehe ya harusi." 5 Lakini
watu hao hawakuzingatia kwa dhati mwaliko wake. Baadhi walirejea katika
mashamba yao, na wengine walirudi katika sehemu zao za biashara. 6 Wengine
waliwainukia watumishi wa mfalme na kuwadharirisha na kuwaua. 7 Lakini mfalme
alikasirika. Alituma jeshi lake, akawaua wale wauaji na kuuteketeza mji wao kwa
moto. 8 Kisha aliwaambia watumishi wake, "Harusi iko tayari, lakini walioalikwa
hawakustahili. 9 Kwa hiyo nendeni kwenye makutano ya njia kuu, waalikeni watu
wengi kadri iwezekanavyo waje kwenye sherehe ya harusi." 10 Watumishi walienda
njia kuu na kuwakaribisha watu wowote waliowaona, wema na wabaya. Hivyo
ukumbi wa harusi ulijaa wageni. 11 Lakini mfalme alipoingia kuwatazama wageni,
alimuona mtu mmoja ambaye hakuvaa vazi rasmi la harusi! 12 Mfalme alimwuliza,
'Rafiki, ulipataje kufika hapa ndani bila vazi la harusi?' Na mtu huyo hakujibu
chochote. 13 Ndipo mfalme alipowaambia watumishi wake, "Mfungeni mtu huyu
mikono na miguu na mtupeni nje katika giza, huko ambako kutakuwa na kilio na
kusaga meno. 14 Kwa kuwa watu wengi wanaitwa, lakini wateule ni wachache."
15 Ndipo Mafarisayo waliondoka na kupanga jinsi ya kumkamata Yesu katika maneno
yake mwenyewe. 16 Ndipo walipowatuma wanafunzi wao pamoja na Maherode. Na
walimwambia Yesu, "Mwalimu, tunajua kuwa wewe ni mtu wa kweli, na kwamba
unafundisha matakwa ya Mungu katika ukweli. Haujali maoni ya mtu mwingine
na hauoneshi upendeleo kwa watu. 17 Kwa hiyo tuambie, unafikiri nini? Je, ni
sahihi kisheria kulipa kodi kwa Kaisari au hapana?" 18 Yesu alifahamu uovu wao
na akasema, "Kwa nini mnanijaribu, enyi wanafiki? 19 Nioneshеni pesa itumikayo
kulipia kodi." Ndipo wakamletea dinari. 20 Yesu akawauliza, "Sura na jina hili ni
vya nani?" 21 Wakamjibu, "Vya Kaisari." Ndipo Yesu akawaambia, "Mpeni Kaisari
vitu vilivyo vyake na vya Mungu mpeni Mungu." 22 Waliposikia hivyo walishangaa.
Kisha walimwacha na kwenda zao. 23 Siku hiyo baadhi ya Masadukayo walikuja kwa
Yesu, wale wasemao kuwa hakuna ufufuo wa wafu. Wakamwuliza, 24 wakisema,

“Mwalimu, Musa alisema, Ikiwa mtu amefariki bila kuzaa watoto, ndugu yake na
amrithi huyo mwanamke na ampatie mtoto kwa ajili ya ndugu yake. 25 Walikuwapo
ndugu saba. Wa kwanza alioa na kisha akafariki bila kuzaa watoto. Akamwachia
mke nduguye. 26 Kisha ndugu yake wa pili naye akafanya vivyo hivyo, kisha yule
wa tatu, ikawa hivyo hadi kwa yule wa saba. 27 Baada ya kufanya hivyo wote,
yule mwanamke naye alifariki. 28 Sasa katika ufufuo huyo mwanamke atakuwa
mke wa nani katika ndugu hao saba? Kwa sababu wote walimuoa.” 29 Lakina Yesu
aliwajibu na kuwaambia, “Mnakosea, kwa sababu hamjui Maandiko wala nguvu za
Mungu. 30 Kwa kuwa katika ufufuo, watu hawaoi wala kuolewa. Badala yake watu
huwa kama malaika huko mbinguni. 31 Lakini kuhusu ufufuo wa wafu, hamjawahi
kusoma kile ambacho Mungu alikisema kwenu, akisema, 32 Mimi ni Mungu wa
Ibrahimu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo? Mungu si Mungu wa wafu,
bali ni Mungu wa walio hai.” 33 Wakati kusanyiko waliposikia hili, waliyashangaa
mafundisho yake. 34 Lakini Mafarisayo waliposikia kuwa Yesu amewanyamazisha
Masadukayo, walijikusanya wao wenyewe kwa pamoja. 35 Mmoja wao, akiwa mwana
sheria, alimwuliza swali kwa kumjaribu. 36 “Mwalimu, ni amri ipi iliyo kuu kuliko
zote katika sheria?” 37 Yesu akamjibu, “Lazima umpende Bwana kwa moyo wako
wote, kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. 38 Hii ndiyo amri iliyo kuu
na ya kwanza. 39 Na ya pili inafanana na hiyo- Ni lazima kumpenda jirani yako
kama unavyojipenda mwenyewe. 40 Sheria zote na Manabii hutegemea amri hizi
mbili.” 41 Na Mafarisayo walipokuwa bado wamejikusanya pamoja, Yesu aliwauliza
swali. 42 Akisema, “J! e, Mwafikiri nini juu ya Kristo? Yeye ni Mwana wa nani?”
Nao wakamjibu, “Ni mwana wa Daudi.” 43 Yesu akawajibu, “Ni kwa namna gani
Daudi katika Roho anamwita Bwana, akisema, 44 'Bwana alimwambia Bwana wangu,
“Kaa mkono wangu wa kuume, hadi nitakapowafanya maadui zako wawekwe chini
ya miguu yako.”'?” 45 Kama Daudi anamwita Kristo “Bwana,” jinsi gani atakuwa
mtoto wake?” 46 Hakuna aliyeweza kumjibu neno tena, na hakuna aliyethubutu tena
kumwuliza maswali zaidi tangu siku hiyo na kuendelea.

## 23

1 Baadaye aliongea na umati wa watu na wanafunzi wake. Akasema, 2 “Waandishi
na Mafarisayo wanakalia kiti cha Musa. 3 Kwa hiyo chochote wanacho waamuru
kufanya, fanyeni huku mkiwachunguza. Lakini msije mkaiga matendo yao, kwa
sababu wao hutamka mambo wasiyoyafanya. 4 Kweli, wao hufunga mizigo mizito
ambayo ni vigumu kuibeba, na kisha huwabebesha watu mabegani mwao. Lakini
wao wenyewe hawasogezi hata kidole kuibeba. 5 Matendo yao yote, huyafanya
ili watazamwe na watu. Kwa sababu wao hupanua masanduku yao na huongeza
ukubwa wa mapindo ya mavazi yao. 6 Wao hupendelea kukaa maeneo ya kifahari
katika sherehe na katika viti vya heshima ndani ya masinagogi, 7 na kusalimiwa
kwa heshima maeneo ya sokoni, na kuitwa “Walimu” na watu. 8 Lakini ninyi
hampaswi kuitwa “Walimu,” Kwa kuwa mnaye Mwalimu mmoja, na ninyi wote ni
ndugu. 9 Msimuite mtu yeyote hapa duniani kuwa baba yenu, kwa kuwa mnaye Baba
mmoja tu, naye yuko mbinguni. 10 Wala msije kuitwa 'walimu,' kwa kuwa mnaye
Mwalimu mmoja tu, yaani Kristo. 11 Bali aliye mkubwa miongoni mwenu atakuwa
mtumishi wenu. 12 Yeyote ajiinuae atashushwa. Na yeyote anaye jishusha atainuliwa.
13 Lakini ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Mnawafungia watu ufalme wa
mbinguni. Nanyi hamwezi kuuingia, na hamwaruhusu wanaoingia kufanya hivyo.
14 (Zingatia: Msitari wa 14 hauonekani katika nakala bora za kale. Baadhi ya nakala
huongeza msitari huu baada ya msitari wa 12. Msitari wa 14 “Ole wenu wandishi na
Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mnawameza wajane”). 15 Ole wenu Waandishi na

Mafarisayo, wanafiki! Mnavuka ngambo ya bahari na kufika kumfanya mtu mmoja
aamini yale mnayoyafundisha, na anapokuwa kama ninyi, mnamfanya mara mbili
mwana wa jehanamu kama ninyi wenyewe mlivyo. 16 Ole wenu viongozi vipofu,
ninyi msemao,, Yeyote aapaye kwa hekalu, si kitu. Lakini anayeapa kwa dhahabu
ya hekalu, amefungwa na kiapo chake. 17 Enyi vipofu wapumbavu, kipi ni kikubwa
kuliko kingine, dhahabu au hekalu ambalo limeweka wakfu dhahabu kwa Mungu?
18 Na, yeyote aapaye kwa madhabahu, si kitu. Bali anayeapa kwa sadaka iliyo juu
yake, amefungwa na kiapo chake. 19 Enyi watu vipofu, kipi ni kikubwa kuliko
kingine, sadaka au madhabahu ambayo huweka wakfu sadaka zinazotolewa kwa
Mungu? 20 Kwa hiyo, yeye aapaye kwa madhabahu huapa kwa hiyo na kwa vitu
vyote vilivyo juu yake. 21 Naye aapaye kwa hekalu, huapa kwa hilo na kwa yeye
akaaye ndani yake. 22 Na yeye aapaye kwa mbingu, huapa kwa kiti cha enzi cha
Mungu na kwa yeye aketie juu yake. 23 Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki!
Kwa kuwa mnalipa zaka kwa bizali, mnaanaa na mchicha, lakini mnaacha mambo
mazito ya sheria- haki, rehema, na imani. Lakini haya mnapaswa kuwa mmeyafanya,
na siyo kuacha mengine bila kuyatekeleza. 24 Enyi viongozi vipofu, ninyi ambao
mnachuja mdudu mdogo lakini mnameza ngamia! 25 Ole wenu, waandishi na
Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnasafisha nje ya vikombe na nje ya sahani,
lakini ndani pamejaa dhuluma na kutokuwa na kiasi. 26 Enyi Mafarisayo vipofu,
safisheni kwanza ndani ya kikombe na ndani ya sahani, ili upande wa nje nao pia
uwe safi. 27 Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnafanana
na makaburi yaliyopakwa chokaa, ambayo kwa nje huonekana mazuri, lakini kwa
ndani yamejaa mifupa ya wafu na kila kitu kilicho kichafu. 28 Vivyo hivyo, nanyi
kwa nje mwaonekana wenye haki mbele ya watu, lakini kwa ndani mmejaa unafiki
na udhalimu. 29 Ole wenu, waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mwajenga
makaburi ya manabii na kuyapamba makaburi ya wenye haki. 30 Ninyi mwasema,
kama tungeishi siku za baba zetu, tusingekuwa tumeshiriki pamoja nao kumwaga
damu za manabii. 31 Kwa hiyo mwajishuhudia wenyewe kwamba ninyi ni watoto
wa hao waliowaua manabii. 32 Pia ninyi mnakamilisha kujaza sehemu inayostahili
dhambi ya baba zenu. 33 Enyi nyoka, wana wa vipiribao, kwa namna gani mtaikwepa
hukumu ya jehanamu? 34 Kwahiyo, tazama, nawatuma kwenu manabii, watu wenye
hekima, na waandishi. Baadhi yao mtawaua na kuwasulibisha. Na baadhi yao
mtawachapa ndani ya masinagogi yenu na kuwafukuza kutoka mji mmoja hadi
mwingine. 35 Matokeo ni kwamba juu yenu patatokea damu zote za wenye haki
zilizomwagwa duniani, kuanzia damu ya Habili mwenye haki hadi kwa damu ya
Zakaria mwana wa Barakia, mliye muua kati ya patakatifu na madhabahu. 36 Kweli,
nawaambieni, mambo haya yote yatakipata kizazi hiki. 37 Yerusalemu, Yerusalemu,
wewe unayewaua manabii na kuwapiga mawe wale ambao wanatumwa kwako!
mara ngapi nimewakusanya watoto wako pamoja kama vile kuku awakusanyavyo
vifaranga wake chini ya mbawa zake, lakini haukukubali! 38 Tazama, nyumba yako
imebaki ukiwa. 39 Nami nakuambia, Kuanzia sasa na kuendelea hautaniona, hadi
utakaposema, 'Amebarikiwa yeye ajaye kwa jina la Bwana.”'

# 24

1 Yesu alitoka hekaluni na kwenda zake. Wanafunzi wake walimwendea na
kumuonesha majengo ya hekalu. 2 Laikni aliwajibu na kuwaambia, “Je, hamuyaoni
mambo haya yote? Kweli nawaambia, hakuna jiwe litalobaki juu ya lingine
bila kubomolewa.” 3 Na alipokaa katika Mlima wa Mizeituni, wanafunzi wake
walimwendea kwa faragha na kusema, “Tuambie, mambo haya yatatokea lini? Kitu
gani kitakuwa dalili ya kuja kwako na mwisho wa ulimwengu?” 4 Yesu aliwajibu

na kuwaambia, “Iweni makini kwamba asije mtu akawapotosha. 5 Kwa kuwa wengi
watakuja kwa jina langu. Watasema, 'Mimi ndiye Kristo', na watawapotosha wengi.
6 Mtasikia vita na taarifa za vita. Angalieni msije mkawa na wasiwasi, kwa kuwa
mambo haya hayabudi kutokea; lakini ule mwisho utakuwa bado. 7 Kwa kuwa
taifa litainuka dhidi ya taifa jingine, na ufalme dhidi ya ufalme. Kutakuwa na
njaa na matetemeko ya ardhi katika sehemu mbalimbali. 8 Lakini mambo haya
yote ni mwanzo tu wa uchungu wa kujifungua. 9 Ndipo watawatoa kwa ajili
ya mateso na kuwaua. Mtachukiwa na mataifa yote kwa sababu ya jina langu.
10 Ndipo wengi watajikwaa na kusalitiana na watachukiana wenyewe kwa wenyewe.
11 Manabii wengi wa uongo watatokea na kuwadanganya wengi. 12 Kwa sababu
uovu utaongezeka, upendo wa wengi utapoa. 13 Lakini atakaye vumilia mpaka
mwisho, ataokolewa. 14 Hii Injili ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu mzima
kama ushuhuda kwa mataifa yote. Na ndipo ule mwisho utafika. 15 Kwa hiyo,
mtakapoona chukizo la uharibifu, lililosemwa na nabii Danieli limesimama mahali
patakatifu [asomaye na afahamu], 16 ndipo walioko Yuda wakimbilie milimani. 17 Na
yule aliyeko juu ya paa la nyumba asiweze kuteremka chini kuchukua kitu chochote
kutoka ndani ya nyumba yake, 18 naye aliyeko shambani asirudi kuchukua vazi lake.
19 Lakini ole wao ambao wana mtoto na wale ambao wananyonyesha katika siku
hizo! 20 Ombeni kwamba kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi, wala siku ya
sabato. 21 Kwa kuwa kutakuwa na dhiki kuu, ambayo haijawahi kuwapo tangu
kuumbwa kwa ulimwengu hadi sasa, na wala haitakuwapo tena. 22 Kama siku hizo
zisingefupishwa, hakuna ambaye angeokoka. Lakini kwa sababu ya wateule, siku
hizo zitafupishwa. 23 Kisha ikiwa mtu yeyote atawaambia 'Tazama, Kristo yuko hapa!
au, 'Kristo yuko kule' msiamini maneno hayo. 24 Kwa kuwa Makristo wa uongo na
manabii wa uongo watakuja na kuonesha ishara kubwa na maajabu, kwa kusudi la
kupotosha, kama ingewezekana hata na wateule. 25 Tazameni, nimewatahadharisha
kabla ya mambo hayo kutokea. 26 Kwa hiyo, ikiwa watawaambia, ''Kristo yuko
jangwani,' msiende huko jangwani. Au, 'Tazameni, yuko ndani ya nyumba,' msiamini
maneno hayo. 27 Kama vile radi inavyomulika kutokea mashariki na kuangaza hadi
magharibi, ndivyo itakavyokuwa kuja kwa Mwana wa Adamu. 28 Popote ulipo mzoga,
huko ndiko tai wakusanyikapo. 29 Lakini mara baada ya dhiki kuu ya siku zile, Jua
litatiwa giza, mwezi hautatoa mwanga wake, nyota zitaanguka kutoka angani, na
nguvu za mbinguni zitatikisika. 30 Ndipo ishara ya Mwana wa Adamu itaonekana
angani, na makabila yote ya dunia wataomboleza. Watamwona Mwana wa Adamu
akija katika mawingu ya angani kwa nguvu na utukufu mkuu. 31 Atawatuma
malaika wake kwa sauti kuu ya tarumbeta, nao watawakusanya pamoja wateule
wake kutoka pande nne za dunia, kutoka mwisho mmoja wa mbingu hadi mwingine.
32 Jifunzeni somo kutokana na mti mtini. Mara tu tawi linapochipuka na kutoa
majani, mnajua kwamba kiangazi kinakaribia. 33 Hivyo pia, mtakapoona mambo
haya yote, mnapaswa kujua kwamba amekaribia, karibu na malango. 34 Kweli
nawaambia, kizazi hiki hakitapita, hadi mambo yote haya yatakuwa yametokea.
35 Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita kamwe. 36 Lakini kuhusu
siku ile na saa hakuna mtu ajuaye, hata malaika wa mbinguni, wala Mwana, bali
Baba peke yake. 37 Kama vile ilivyokuwa katika siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa
kuja kwa Mwana wa Adamu. 38 Kwa kuwa katika siku hizo kabla ya gharika
watu walikuwa wakila na kunywa, wakioa na kuolewa hadi siku ile ambayo Nuhu
aliingia katika safina, 39 na hawakujua kitu chochote hadi gharika ilipokuja na
kuwasomba wote - ndivyo itakavyokuwa kuja kwa Mwana wa Adamu. 40 Ndipo
watu wawili watakuwa shambani- mmoja atachukuliwa, na mmoja ataachwa nyuma.
41 Wanawake wawili watakuwa wanasaga pamoja - mmoja atachukuliwa, na mmoja

atabaki. 42 Kwa hiyo, kuweni macho kwa sababu hamjui ni siku gani ambayo atakuja
Bwana wenu. 43 Lakini mjue kwamba, ikiwa bwana mwenye nyumba angejua ni saa
ipi ambayo mwizi angekuja, angekesha na asingeruhusu nyumba yake kuvamiwa.
44 Kwa hiyo, pia mnapaswa kuwa tayari, kwa kuwa Mwana wa Adamu atakuja katika
saa msiyoitarajia. 45 Hivyo ni nani aliye mwaminifu, mtumwa mwenye akili, ambaye
bwana wake amempa madaraka juu ya walio katika nyumba yake, ili awape chakula
kwa wakati unaofaa? 46 Amebarikiwa mtumishi huyo, ambaye bwana wake atamkuta
akifanya hivyo wakati ajapo. 47 Kweli nawaambia kwamba bwana atamweka juu ya
kila kitu kilicho chake. 48 Lakini kama mtumwa mwovu akisema moyoni mwake,
'Bwana wangu amekawia,' 49 na akaanza kuwapiga watumishi wake, na akala na
kulewa vileo, 50 Bwana wa mtumwa huyo atakuja katika siku ambayo haitarajii, na
katika saa ambayo haijui. 51 Bwana wake atamkata vipande viwili na kumweka katika
nafasi moja sawa na wanafiki, ambako kutakuwa na kilio na kusaga meno.

# 25

1 Ndipo ufalme wa mbinguni utafananishwa na wanawali kumi waliochukua
taa zao na kuondoka kwenda kumpokea bwana harusi. 2 Watano miongoni
mwao walikuwa wapumbavu na watano wengine walikuwa werevu. 3 Wanawali
wapumbavu walipochukua taa zao, hawakuchukua mafuta yoyote. 4 Bali wanawali
welevu walichukua vyombo vyenye mafuta pamoja na taa zao. 5 Sasa wakati bwana
harusi amechelewa kufika, wote walishikwa usingizi na wakalala. 6 Lakini wakati
wa usiku wa manane kulikuwa na yowe, 'Tazama, bwana harusi! Tokeni nje
mkampokee.' 7 Ndipo hao wanawali waliamka wote na kuwasha taa zao. 8 Wale
wapumbavu waliwaambia wale welevu, 'Mtupatie sehemu ya mafuta yenu kwa
sababu taa zetu zinazimika.' 9 Lakini wale welevu waliwajibu na kuwaambia, 'Kwa
kuwa hayatatutosha sisi na ninyi, badala yake nendeni kwa wanaouza mjinunulie
kiasi kwa ajili yenu.' 10 Wakati wameenda huko kununua, Bwana harusi alifika,
na wote waliokuwa tayari walienda naye kwenye sherehe ya harusi, na mlango
ulifungwa. 11 Baadaye wale wanawali wengine pia walifika na kusema, 'Bwana,
bwana, tufungulie.' 12 Lakini alijibu na kusema, 'Kweli nawaambia, Mimi siwajui.'
13 Kwa hiyo angalieni, kwa kuwa hamjui siku au saa. 14 Kwa kuwa ni sawa na mtu
alipotaka kusafiri kwenda nchi nyingine. Aliwaita watumwa wake na kuwakabidhi
utajiri wake. 15 Mmoja wao alimpatia talanta tano, mwingine alimpa mbili, na yule
mwingine alimpa talanta moja. Kila mmoja alipokea kiasi kulingana na uwezo wake,
na yule mtu alisafari kwenda zake. 16 Mapema yule aliyepokea talanta tano alienda
kuziwekeza, na kuzalisha talanta zingine tano. 17 Vilevile yule aliyepokea talanta
mbili, alizalisha zingine mbili. 18 Lakini mtumwa aliyepokea talanta moja, alienda
zake, akachimba shimo ardhini, na kuificha fedha ya bwana wake. 19 Na baada ya
muda mrefu, bwana wa watumwa hao alirudi na kutengeneza mahesabu nao. 20 Yule
mtumwa aliyepokea talanta tano alikuja na kuleta talanta zingine tano, akasema,
'Bwana, ulinipa talanta tano. Tazama, nimepata faida ya talanta zingine tano.'
21 Bwana wake alimwambia, 'Hongera, mtumwa mzuri na mwaminifu! Umekuwa
mwaminifu kwa vitu vidogo. Nitakupa madaraka juu ya vitu vingi. Ingia katika
furaha ya bwana wako.' 22 Mtumwa aliyepokea talanta mbili alikuja na kusema,
'Bwana, ulinipa talanta mbili. Tazama, nimepata faida ya talanta zingine mbili,'
23 Bwana wake alimwambia, 'Hongera, mtumwa mzuri na mwaminifu! Umekuwa
mwaminifu kwa vitu vichache. Nitakupa madaraka juu ya vitu vingi. Ingia katika
furaha ya bwana wako.' 24 Baadaye mtumwa aliyepokea talanta moja alikuja na
kusema, 'Bwana, najua kuwa wewe ni mtu mkali. Unachuma mahali ambapo
hukupanda, na unavuna mahali ambapo hukusia. 25 Mimi niliogopa, nikaenda

zangu na kuificha talanta yako katika udongo. Tazama, unayo hapa ile iliyo yako.'
26 Lakini bwana wake alijibu na kusema, 'Wewe mtumwa mwovu na mzembe, ulijua
kwamba ninachuma mahali ambapo sijapanda na kuvuna mahali ambapo sikusia.
27 Kwahiyo ulipaswa kuwapa fedha yangu watu wa benki, na wakati wa kurudi
kwangu ningeipokea ile yangu pamoja na faida. 28 Kwa hiyo mnyang'anyeni hiyo
talanta na mpeni yule mtumwa aliye na talanta kumi. 29 Kila mtu aliye nacho,
ataongezewa zaidi-hata kwa kuzidishiwa sana. Lakini kwa yeyote asiye na kitu, hata
alicho nacho atanyang'anywa. 30 Mtupeni nje gizani huyo mtumwa asiyefaa, ambako
kutakuwa na kilio na kusaga meno.' 31 Wakati Mwana wa Adamu atakapokuja katika
utukufu wake, na malaika wote pamoja naye, ndipo atakapokaa juu ya kiti chake
cha utukufu. 32 Mataifa yote yatakusanyika mbele zake, naye atawatenganisha watu,
kama vile mchungaji anavyowatenganisha kondoo na mbuzi. 33 Atawaweka kondoo
mkono wake wa kuume, bali mbuzi atawaweka mkono wa kushoto. 34 Kisha mfalme
atawaambia wale walio mkono wake wa kulia, 'Njoni, mliobarikiwa na Baba yangu,
urithini ufalme ulioandaliwa kwa ajili yenu tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu.
35 Kwa kuwa nilikuwa na njaa na mlinipa chakula; Nilikuwa mgeni na mlinikaribisha;
36 Nilikuwa uchi, na mlinivika nguo; Nilikuwa mgonjwa na mkanitunza; Nilikuwa
kifungoni na mkaniijia.' 37 Ndipo wenye haki watamjibu na kumwambia, 'Bwana,
lini tulikuona ukiwa na njaa, na kukulisha? Au una kiu na tukakupa maji? 38 Na
lini tulikuona ukiwa mgeni, na tukakukaribisha? Au ukiwa uchi na tukakuvisha
nguo? 39 Na lini tulikuona ukiwa mgonjwa, au katika kifungo, na tukakujia? 40 Na
mfalme atawajibu na kuwaambia, 'Kweli nawaambia, mlichotenda hapa kwa mmoja
wa ndugu zangu wadogo, mlinitendea mimi.' 41 Ndipo atawaambia hao walio mkono
wake wa kushoto, 'Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, nendeni katika moto wa milele
ulioandaliwa kwa ajili ya shetani na malaika zake, 42 kwa sababu nilikuwa na njaa
lakini hamkunipa chakula; Nilikuwa na kiu lakini hamkunipa maji; 43 Nilikuwa mgeni
lakini hamkunikaribisha; nikiwa uchi lakini hamkunipa mavazi; nikiwa mgonjwa na
nikiwa kifungoni, lakini hamkunitunza.' 44 Ndipo wao pia watamjibu na kusema,
'Bwana, lini tulikuona ukiwa na njaa, au una kiu, au u mgeni, au ukiwa uchi, au
ukiwa mgonjwa, au ukiwa mfungwa, na hatukukuhudumia? 45 Kisha atawajibu na
kusema, 'Kweli nawaambia, kile ambacho hamkutenda kwa mmoja wa hawa wadogo,
hamkunitendea mimi.' 46 Hawa watakwenda katika adhabu ya milele bali wenye haki
katika uzima wa milele.”

## 26

1 Wakati Yesu alipomaliza kusema maneno yote hayo, aliwaambia wanafunzi wake,
2 “Mnajua kwamba baada ya siku mbili kutakuwa na sikukuu ya pasaka, na mwana
wa Adamu atatolewa ili asulibiwe.” 3 Baadaye wakuu wa makuhani na wazee wa
watu walikutana pamoja katika makao ya Kuhani Mkuu, aliye kuwa anaitwa Kayafa.
4 Kwa pamoja walipanga njama ya kumkamata Yesu kwa siri na kumuua. 5 Kwa
kuwa walisema, “Isifanyike wakati wa sikukuu, kusudi isije ikazuka ghasia miongoni
mwa watu.” 6 Wakati Yesu alipokuwa Bethania katika nyumba ya Simoni mkoma,
7 alipokuwa amejinyoosha mezani, mwanamke mmoja alikuja kwake akiwa amebeba
mkebe wa alabasta iliyokuwa na mafuta yenye thamani kubwa, na aliyamimina
juu ya kichwa chake. 8 Lakini wanafunzi wake walipoona jambo hilo, walichukia
na kusema, “Nini sababu ya hasara hii? 9 Haya yangeweza kuuzwa kwa kiasi
kikubwa na kupewa maskini.” 10 Lakini Yesu, akiwa anajua hili, aliwaambia, “Kwa
nini mnamsumbua mwanamke huyu? Kwa kuwa amefanya kitu kizuri kwangu.
11 Masikini mnao siku zote, lakini hamtakuwa pamoja nami daima. 12 Kwa sababu
alipomimina mafuta haya juu ya mwili wangu, alifanya hivyo kwa ajili ya maziko

yangu. 13 Kweli nawaambieni, popote Injili hii itakapohubiriwa katika ulimwengu
mzima, kitendo alichofanya huyu mwanamke, pia kitakuwa kinasemwa kwa ajili ya
kumkumbuka.” 14 Ndipo mmoja wa wale Kumi na wawili, aliyeitwa Yuda Iskariote,
alienda kwa wakuu wa makuhani 15 na kusema, “Mtanipatia nini nikimsaliti?”
Wakampimia Yuda vipande thelathini vya fedha. 16 Tangu muda huo alitafuta
nafasi ya kumsaliti. 17 Hata siku ya kwanza ya mikate isiyotiwa chachu, wanafunzi
walimwendea Yesu na kusema, “Wapi unataka tukuandalie ule chakula cha Pasaka?”
18 Akawaambia, “Nendeni mjini kwa mtu fulani na mwambieni, Mwalimu anasema,
“Muda wangu umekaribia. Nitaitimiza Pasaka pamoja na wanafunzi wangu katika
nyumba yako.”” 19 Wanafunzi walifanya kama Yesu alivyowaagiza, na waliandaa
chakula cha Pasaka. 20 Ilipofika jioni, aliketi kula chakula pamoja na wale wanafunzi
Kumi na Wawili. 21 Walipokuwa wanakula chakula, alisema, “Kweli nawaambia
kwamba mmoja wenu atanisaliti.” 22 Walihuzunika sana, na kila mmoja alianza
kumuuliza, “Je, hakika siyo mimi, Bwana?” 23 Akawajibu, “Yule ambaye anachovya
mkono wake pamoja nami katika bakuli ndiye atakaye nisaliti. 24 Mwana wa
Adamu ataondoka, kama alivyoandikiwa. Lakini ole wake mtu ambaye atamsaliti
Mwana wa Adamu! Ingekuwa vizuri kwa mtu huyo kama asingezaliwa.” 25 Yuda,
ambaye angemsaliti alisema, “Je!, Ni mimi Rabi?” Yesu akamwambia, “Umesema
jambo hilo wewe mwenyewe.” 26 Walipokuwa wakila chakula, Yesu aliutwaa
mkate, akaubariki, na kuumega. Akawapa wanafunzi wake akisema, “Chukueni,
mle. Huu ni mwili wangu.” 27 Akatwaa kikombe na kushukuru, akawapa na
kusema, “Kunyweni wote katika hiki. 28 Kwa kuwa hii ni damu ya agano langu,
inayomwagwa kwa ajili ya wengi kwa msamaha wa dhambi. 29 Lakini nawaambieni,
sitakunywa tena matunda ya mzabibu huu, hadi siku ile nitakapokunywa mpya
pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu.” 30 Walipokuwa wamemaliza kuimba
wimbo, walitoka kwenda Mlima wa Mizeituni. 31 Kisha Yesu aliwaambia, “Usiku
huu ninyi nyote mtajikwaa kwa sababu yangu, kwa kuwa imeandikwa, Nitampiga
mchungaji na kondoo wa kundi watatawanyika. 32 Lakini baada ya kufufuka kwangu,
nitawatangulia kwenda Galilaya.” 33 Lakini Petro alimwambia, “Hata kama wote
watakukataa kwa sababu ya mambo yatakayokupata, mimi sitakukataa.” 34 Yesu
akamjibu, “kweli nakuambia, usiku huu kabla jogoo hajawika, utanikana mara
tatu.” 35 Petro akamwambia, “hata kama ingenipasa kufa na wewe, sitakukana.”
Na wanafunzi wengine wote wakasema vivyo hivyo. 36 Baadaye Yesu alienda
nao mahali panapoitwa Gethsemane na aliwaambia wanafunzi wake, “Kaeni hapa
wakati nikienda huko na kuomba.” 37 Akamchukua Petro na wana wawili wa
Zebedayo na akaanza kuhuzunika na kusononeka. 38 Kisha aliwaambia, “Roho
yangu ina huzuni kubwa sana, hata kiasi cha kufa. Bakini hapa na mkeshe pamoja
nami.” 39 Akenda mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, na kuomba. Akasema, “Baba
yangu, kama inawezekana, kikombe hiki kiniepuke. Isiwe kama ninavyotaka mimi,
bali kama utakavyo wewe.” 40 Akawaendea wanafunzi na akawakuta wamelala
usingizi, na akamwambia Petro, “Kwa nini hamkuweza kukesha nami kwa saa moja?
41 Kesheni na kuomba kusudi msiingie majaribuni. Roho i radhi, lakini mwili ni
dhaifu.” 42 Akaenda zake mara ya pili na kuomba, akasema, “Baba yangu, kama
jambo hili haliwezi kuepukika na ni lazima nikinywee kikombe hiki, mapenzi yako
yatimizwe.” 43 Akarudi tena na kuwakuta wamelala usingizi, kwa kuwa macho
yao yalikuwa mazito. 44 Kisha akawaacha tena akaenda zake. Akaomba mara ya
tatu akisema maneno yaleyale. 45 Baadaye Yesu aliwaendea wanafunzi wake na
kuwaambia, “Bado mmelala tu na kujipumzisha? Tazameni, saa imekaribia, na
Mwana wa Adamu anasalitiwa mikononi mwa wenye dhambi. 46 Amkeni, tuondoke.
Tazama, yule anaye nisaliti amekaribia.” 47 Wakati alipokuwa bado anaongea,

Yuda mmoja wa wale Kumi na Wawili, akafika. Kundi kubwa lilifika pamoja naye
likitokea kwa wakuu wa makuhani na wazee wa watu. Walikuja na mapanga
na marungu. 48 Tena mtu aliyekusudia kumsaliti Yesu alikuwa amewapa ishara,
akisema, "Yule nitakayembusu, ndiye yeye. Mkamateni." 49 Mara hiyo alikuja
kwa Yesu na kusema, "Salamu, Mwalimu!" Na akambusu. 50 Yesu akamwambia,
"Rafiki, lifanye lile ambalo limekuleta." Ndipo wakaja, na kumnyooshea mikono
Yesu, na kumkamata. 51 Tazama, mtu mmoja aliyekuwa pamoja na Yesu, alinyosha
mkono wake, akachomoa upanga wake, na akampiga mtumishi wa kuhani mkuu, na
kumkata sikio lake. 52 Ndipo Yesu akamwambia, rudisha upanga wako pale ulipoutoa,
kwa kuwa wote watumiao upanga wataangamizwa kwa upanga. 53 Mnadhani kuwa
siwezi kumwita Baba yangu, naye akanitumia majeshi zaidi ya kumi na mawili
ya malaika? 54 Lakini basi jinsi gani maandiko yangeweza kutimizwa, hivi ndivyo
inapasa kutokea?" 55 Wakati huo Yesu akauambia umati, "Je! Mmekuja na mapanga
na marungu kunikamata kama mnyang'anyi? Kila siku nilikaa hekaluni nikifundisha,
na hamkunishika! 56 Lakini yote haya yametendeka ili Maandiko ya manabii
yatimie." Ndipo wanafunzi wake wakamwacha na kukimbia. 57 Wale waliomkamata
Yesu alimpeleka kwa Kayafa, Kuhani Mkuu, mahali ambapo waandishi na wazee
walikuwa wamekusanyika pamoja. 58 Lakini Petro alimfuata nyuma kwa mbali hadi
katika ukumbi wa Kuhani Mkuu. Aliingia ndani na kukaa pamoja na walinzi aone
kitakachotokea. 59 Basi wakuu wa makuhani na Baraza lote walikuwa wakitafuta
ushahidi wa uongo dhidi ya Yesu, kusudi wapate kumuua. 60 Ingawa walijitokeza
mashahidi wengi, Lakini hawakupata sababu yoyote. Lakini baadaye mashahidi
wawili walijitokeza mbele 61 na kusema, " Mtu huyu alisema, ''Naweza kulivunja
hekalu la Mungu na kulijenga tena kwa siku tatu."' 62 Kuhani Mkuu alisimama na
kumwuliza, "Hauwezi kujibu? Hawa wanakushuhudia nini dhidi yako?" 63 Lakini
Yesu alikaa kimya. Kuhani Mkuu akamwambia, "Kama Mungu aishivyo, nakuamuru
utwambie, kama wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu." 64 Yesu akamjibu, "Wewe
mwenyewe umesema jambo hilo. Lakini nakuambia, toka sasa na kuendelea
utamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kulia wenye Nguvu, na akija
katika mawingu ya mbinguni." 65 Ndipo Kuhani Mkuu alirarua mavazi yake na
kusema, "Amekufuru! Je, twahitaji tena ushahidi wa nini? Angalia, tayari mmesikia
akikufuru. 66 Je! Mnawaza nini? Wakajibu na kusema, "Anastahili kifo." 67 Kisha
walimtemea mate usoni na kumpiga ngumi, na kumchapa makofi kwa mikono yao,
68 na kusema, "Tutabirie, wewe Kristo. Ni nani amekuchapa?" 69 Wakati huo Petro
alikuwa amekaa nje katika ukumbi, na mtumishi wa kike alimwendea na kusema,
"Wewe pia ulikuwa pamoja na Yesu wa Galilaya." 70 Lakini alikana mbele yao wote,
akisema, Sijui kitu unachosema." 71 Alipoenda nje ya lango, mtumishi mwingine wa
kike alimwona na kuwaambia waliokuwepo hapo, "Mtu huyu pia alikuwa pamoja na
Yesu wa Nazareti." 72 Akakana tena kwa kiapo, "Mimi simjui mtu huyu." 73 Muda
mfupi baadaye, wale waliokuwa wamesimama karibu, walimwendea na kusema na
Petro, "Kwa hakika wewe pia ni mmoja wao, kwa kuwa hata lafudhi yako inaonesha."
74 Ndipo alianza kulaani na kuapa, "Mimi simfahamu mtu huyu," na mara hiyo jogoo
akawika. 75 Petro alikumbuka maneno aliyoambiwa na Yesu, "Kabla jogoo hajawika
utanikana mara tatu."

## 27

1 Muda wa asubuhi ulipofika, wakuu wote wa makuhani na wazee wa watu
walikula njama dhidi ya Yesu wapate kumuua. 2 Walimfunga, walimwongoza, na
kumfikisha kwa Liwali Pilato. 3 Kisha wakati Yuda, ambaye alikuwa amemsaliti,

aliona kwamba Yesu amekwisha kuhukumiwa, alijuta na kurudisha vipande the-
lathini vya fedha kwa mkuu wa makuhani na wazee, [4] na akasema, "Nimefanya
dhambi kwa kuisaliti damu isiyo na hatia." Lakini wakajibu, "Inatuhusu nini
sisi? Yaangalie hayo mwenyewe." [5] Kisha alivirusha chini vile vipande vya fedha
katika hekalu, na kuondoka zake na kujinyonga mwenyewe. [6] Mkuu wa makuhani
alivichukua vile vipande vya fedha na kusema, "Si halali kuiweka fedha hii katika
hazina, kwa sababu ni gharama ya damu." [7] Walijadiliana kwa pamoja na fedha
ikatumika kununulia shamba la mfinyazi la kuzika wageni. [8] Kwa sababu hii shamba
hilo limekuwa likiitwa, "Shamba la damu" hadi leo hii. [9] Kisha lile neno lililokuwa
limenenwa na nabii Yeremia lilitimia, kusema, "Walitwaa vipande thelathini vya
fedha, gharama iliyopangwa na watu wa Israel kwa ajili yake, [10] na waliitumia
kwa shamba la mfinyanzi, kama Bwana alivyokuwa amenielekeza." [11] Sasa Yesu
alisimama mbele ya liwali, na liwali akamwuliza, "Je! Wewe ni mfalme wa
Wayahudi?" Yesu alimjibu, "Wewe wasema hivyo." [12] Lakini wakati aliposhitakiwa
na wakuu wa makuhani na wazee, hakujibu chochote. [13] Kisha Pilato alimwambia,
"Hujayasikia mashitaka yote dhidi yako?" [14] Lakini hakumjibu hata neno moja,
hivyo liwali alijawa na mshangao. [15] Sasa katika sikukuu ilikuwa desturi ya liwali
kumfungua mfungwa mmoja anayechaguliwa na umati. [16] Wakati huo walikuwa
na mfungwa sugu jina lake Baraba. [17] Hivyo wakati walipokuwa wamekusanyika
pamoja, Pilato aliwauliza, "Ni nani mnataka tumfungue kwa ajili yenu?" Baraba
au Yesu anayeitwa Kristo?" [18] Kwa sababu alijua kwamba wamekwisha kumkamata
kwa sababu ya chuki. [19] Wakati alipokuwa akiketi kwenye kiti chake cha hukumu,
mke wake alimtumia neno na kusema, "Usitende jambo lolote kwa mtu huyo
asiye na hatia. Kwani nimeteswa mno hata leo katika ndoto kwa sababu yake."
[20] Ndipo wakuu wa makuhani na wazee waliwashawishi makutano wamwombe
Baraba, na Yesu auawe. [21] Liwali aliwauliza, "Ni yupi kati ya wawili mnataka mimi
nimwachie kwenu?" Walisema, "Baraba." [22] Pilato akawaambia, "Nimtendee nini
Yesu anayeitwa Kristo?" Wote wakajibu, "Msulibishe" [23] Naye akasema, "Kwa nini,
ni kosa gani ametenda?" Lakini walizidi kupaza sauti hata juu mno, "Msulibishe."
[24] Hivyo wakati Pilato alipoona hawezi kufanya lolote, lakini badala yake vurugu
zilikuwa zimeanza, alitwaa maji akanawa mikono yake mbele ya umati, na kusema,
"Mimi sina hatia juu ya damu ya mtu huyu asiye na hatia. Yaangalieni haya
wenyewe." [25] Watu wote wakasema, "Damu yake iwe juu yetu na watoto wetu."
[26] Kisha akamfungulia Baraba kwao, lakini alimpiga mijeredi Yesu na kumkabidhi
kwao kwenda kusulibiwa. [27] Kisha askari wa liwali wakamchukua Yesu mpaka
Praitorio na kundi kubwa la maaskari wote wakamkusanyika. [28] Wakamvua nguo
zake na kumvika kanzu ya rangi nyekundu. [29] Kisha wakatengeneza taji ya miiba
na kuiweka juu ya kichwa chake, na walimwekea mwanzi katika mkono wake wa
kuume. Walipiga magoti mbele yake na kumkejeri, wakisema, "Salamu, Mfalme wa
Wayahudi?" [30] Na walimtemea mate, na walitwaa mwanzi na kumpiga kichwani.
[31] Wakati walipokuwa wakimkejeri, walimvua ile kanzu na kumvika nguo zake,
na kumwongoza kwenda kumsulibisha. [32] Walipotoka nje, walimwona mtu kutoka
Krene jina lake Simeoni, ambaye walimlazimisha kwenda nao ili apate kuubeba
msalaba wake. [33] Walipofika mahali paitwapo Galigotha, maana yake, "Eneo la fuvu
la Kichwa." [34] Walimpa siki iliyochanganywa na nyongo anywe. Lakini alipoionja,
hakuweza kuinywa. [35] Wakati walipokuwa wamemsulibisha, waligawana mavazi
yake kwa kupiga kura. [36] Na waliketi na kumwangalia. [37] Juu ya kichwa chake
waliweka mashitaka dhidi yake yakisomeka, "Huyu ni Yesu, mfalme wa Wayahudi."
[38] Wanyang'anyi wawili walisulibiwa pamoja naye, mmoja upande wa kulia wake
na mwingine wa kushoto. [39] Wale waliokuwa wakipita walimdhihaki, wakitikisa

vichwa vyao 40 na kusema, “Wewe uliyekuwa unataka kuliharibu hekalu na kulijenga
katika siku tatu, jiokoe mwenyewe! Kama ni Mwana wa Mungu, shuka chini utoke
msalabani!” 41 Katika hali ile ile wakuu wa makuhani walikuwa wakimkashifu,
pamoja na waandishi na wazee, na kusema, 42 “Aliokoa wengine, lakini hawezi
kujiokoa mwenyewe. Yeye ni Mfalme wa Wayahudi. Na ashuke chini toka msalabani,
ndipo tutakapomwamini. 43 Alimtumaini Mungu. Acha Mungu amwokoe sasa kama
anataka, kwa sababu alisema, 'Mimi ni Mwana wa Mungu.'” 44 Na wale wanyang'anyi
waliokuwa wamesulibiwa pamoja naye pia walisema maneno ya kumdhihaki. 45 Sasa
kutoka saa sita kulikuwa na giza katika nchi yote hadi saa tisa. 46 Ilipofika saa tisa,
Yesu akalia kwa sauti kuu, “Eloi, Eloi, lama thabakithan?” akimaanisha, “Mungu
wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha?” 47 Wakati huo baadhi yao waliokuwa
wamesimama pale walisikia, wakasema, “Anamwita Eliya.” 48 Mara moja mmoja
wao alikimbia kuchukua sifongo na kuijaza kinywaji kichungu, akaiweka juu ya
mti na kumpa apate kunywa. 49 Nao waliosalia wakasema, “Mwacheni peke yake,
acheni tuone kama Eliya atakuja kumwokoa.” 50 Kisha Yesu akalia tena kwa sauti
kuu na akaitoa roho yake. 51 Tazama, Pazia la hekalu lilipasuka sehemu mbili
kutokea juu hadi chini. Na ardhi ikatetemeka na miamba ikapasuka vipande.
52 Makaburi yalifunguka, na miili ya watakatifu wengi waliokuwa wamelala usingizi
walifufuliwa. 53 Walitoka kwenye makaburi baada ya ufufuo wake, waliingia mji
mtakatifu, na wakaonekana na wengi. 54 Basi yule akida na wale ambao walikuwa
wakimtazama Yesu waliona tetemeko na mambo yaliyokuwa yakitokea, walijawa
na woga sana na kusema, “Kweli huyu alikuwa Mwana wa Mungu.” 55 Wanawake
wengi waliokuwa wakimfuata Yesu kutoka Galilaya ili kumhudumia walikuwa pale
wakitazama kutoka kwa mbali. 56 Miongini mwao walikuwa Mariamu Magdarena,
Mariamu mama yake Yakobo na Joseph, na mama wa watoto wa Zebedayo 57 Ilipofika
jioni, alikuja mtu tajiri kutoka Arimathayo, aliyeitwa Yusufu, ambaye pia alikuwa
mwanafunzi wa Yesu. 58 Alimwendea Pilato na kuuomba mwili wa Yesu. Kisha
Pilato aliagiza apate kupewa. 59 Yusufu aliuchukua mwili akaufunga na nguo ya
sufi safi, 60 na akaulaza katika kaburi jipya lake alilokuwa amelichonga mwambani.
Kisha akavingirisha jiwe kubwa likafunika mlango wa kaburi na akaenda zake.
61 Mariamu Magdalena na Mariamu mwingine walikuwa pale, wamekaa kuelekea
kaburi. 62 Siku iliyofuata ambayo ilikuwa siku baada ya maandalio, wakuu wa
makuhani na Mafarisayo walikusanyika pamoja kwa Pilato. 63 Wakamwambia,
“Bwana, tunakumbuka kuwa wakati yule mdanganyifu alipokuwa hai, alisema,
'Baada ya siku tatu atafufuka tena.' 64 Kwahiyo, agiza kwamba kaburi lilindwe salama
mpaka siku ya tatu. Vinginevyo, wanafunzi wake wanaweza kuja kumwiba na
kusema kwa watu, 'Amefufuka kutoka wafu.' Na udanganyifu wa mwisho utakuwa
mbaya kuliko ule wa kwanza.” 65 Pilato akawaambia, “Chukueni walinzi. Nendeni
mkafanye hali ya usalama kama muwezavyo.” 66 Hivyo walikwenda na kufanya
kaburi kuwa salama, jiwe liligongwa mhuri na kuweka walinzi.

# 28

1 Baadaye jioni siku ya Sabato, jua lilipokuwa likichwa kuelekea siku ya kwanza
ya juma, Mariamu magadalena, na yule Mariam mwingine walikuja kuliona kaburi.
2 Tazama kulikuwa na tetemeko kubwa, kwa sababu malaika wa Bwana alishuka
na kulivingirisha lile jiwe, kisha akalikalia. 3 Sura yake ilikuwa kama ya umeme,
na mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji. 4 Wale walinzi walijawa na hofu
na kuwa kama wafu. 5 Yule malaika akawafafanulia wale wananawake akisema,
“msiogope kwa maana najua kuwa mnamtafuta Yesu, aliyesulibiwa. 6 Hayupo hapa,
lakini amefufuka kama alivyowaambia. Njooni muone mahali ambapo Bwana alilala.

7 Nendeni haraka mkawaambie wanafunzi wake, 'Amefufuka toka wafu, tazama
amewatangulia Galilaya. Huko ndiko mtamwona.' Tazama mimi nimewaambia.”
8 Wale wanawake waliondoka pale kaburini haraka wakiwa na hofu na furaha
kubwa, na wakakimbia kuwaambia wanafunzi wake. 9 Tazama Yesu akakutana nao
na kusema, “Salamu.”wale wanawake walikuja na kushika miguu yake, na kisha
wakamwabudu. 10 Kisha Yesu akawaambia, “msiogope, nendeni mkawaambie ndugu
zangu watangulie Galilaya. Huko wataniona. 11 Wakati wale wanawake walipokuwa
wakienda, tazama baadhi ya walinzi walienda mjini na kuwaambia wakuu wa
makuhani mambo yote yaliyokuwa yametokea. 12 Nao makuhani walipokuwa
wamekutana na wazee na kulijadili jambo hilo pamoja nao, walitoa kiasi kikubwa
cha pesa kwa wale askari 13 na kuwaambia, “Waambieni wengine kuwa, 'wanafunzi
wa Yesu walikuja usiku wakauiba mwili wa Yesu wakati sisi tulipokuwa tumelala.'
14 Kama taarifa hii itamfikia liwali, sisi tutamshawishi na kuwaondoleeni ninyi
mashaka yote.” 15 Kwa hiyo wale askari wakazichukua zile pesa na kufanya kama
walivyokuwa wameelekezwa. Habari hii ikaenea sana kwa Wayahudi na imekuwa
hivyo hadi leo. 16 Lakini wale mitume kumi na mmoja walienda Galilaya, kwenye ule
mlima aliokuwa amewaelekeza. 17 Nao walipomwona, walimwabudu. lakini baadhi
yao waliona shaka. 18 Yesu akaja kwao akawambia akisema, “Nimepewa mamlaka
yote duniani na mbinguni. 19 Kwa hiyo enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa
wanafunzi. Wabatizeni katika jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtatkatifu.
20 Wafundisheni kuyatii mambo yote niliyowaamuru, Na tazama, mimi niko pamoja
nanyi daima, hata mpaka mwisho wa dunia.

# Marko

1 Huu ni mwanzo wa injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. 2 Kama
ilivyoandikwa na nabii Isaya, “Tazama, ninamtuma mjumbe wangu mbele yako,
mmoja atakayetayarisha njia yako. 3 Sauti ya mtu aitaye nyikani, “Ikamilisheni njia
ya Bwana; zinyosheni njia zake”. 4 Yohana alikuja, akibatiza nyikani na kuhubiri
ubatizo wa toba kwa msamaha wa dhambi. 5 Nchi yote ya Yudea na watu wote wa
Yerusalemu walikwenda kwake. Walikuwa wakibatizwa naye katika mto Yordani,
wakiungama dhambi zao. 6 Yohana alikuwa anavaa vazi la manyoya ya ngamia
na mkanda wa ngozi kiunoni mwake, na alikuwa anakula nzige na asali ya porini.
7 Alihubiri na kusema, “Yupo mmoja anakuja baada yangu mwenye nguvu zaidi
kuliko mimi, na sina hadhi hata ya kuinama chini na kufungua kamba za viatu vyake.
8 Mimi niliwabatiza kwa maji, lakini yeye atawabatiza ninyi kwa Roho Mtakatifu.”
9 Ilitokea katika siku hizo kwamba Yesu alikuja kutoka Nazareti ya Galilaya, na
alibatizwa na Yohana katika mto Yordani. 10 Wakati Yesu alipoinuka kutoka majini,
aliona mbingu zimegawanyika wazi na Roho akishuka chini juu yake kama njiwa.
11 Na sauti ilitoka mbinguni, “Wewe ni Mwanangu mpendwa. Ninapendezwa sana
na wewe.” 12 Kisha mara moja Roho akamlazimisha kwenda nyikani. 13 Alikuwako
nyikani siku arobaini, akijaribiwa na Shetani. Alikuwa pamoja na wanyama wa
mwituni, na malaika walimhudumia. 14 Sasa baada ya Yohana kukamatwa, Yesu
alikuja Galilaya akitangaza injili ya Mungu, 15 akisema, “Muda umetimia, na ufalme
wa Mungu umekaribia. Tubuni na kuamini katika injili”. 16 Na akipita kando
ya bahari ya Galilaya, alimwona Simoni na Andrea ndugu wa Simoni wakitupa
nyavu zao katika bahari, kwa kuwa walikuwa wavuvi. 17 Yesu aliwaambia, “Njoni,
nifuateni, na nitawafanya wavuvi wa watu.” 18 Na mara moja waliacha nyavu na
wakamfuata. 19 Wakati Yesu alipotembea umbali kidogo, alimwona Yakobo mwana
wa Zebedayo na Yohana ndugu yake; walikuwa kwenye mtumbwi wakitengeneza
nyavu. 20 Mara aliwaita na wao walimwacha baba yao Zebedayo ndani ya mtumbwi
na watumishi waliokodiwa, wakamfuata. 21 Na walipofika Kaperinaumu, siku ya
Sabato, Yesu aliingia kwenye sinagogi na kufundisha. 22 Walilishangaa fundisho
lake, kwa vile alikuwa akiwafundisha kama mtu ambaye ana mamlaka na siyo
kama waandishi. 23 Wakati huo huo kulikuwa na mtu katika sinagogi lao aliyekuwa
na roho mchafu, na alipiga kelele, 24 akisema, “Tuna nini cha kufanya na wewe,
Yesu wa Nazareti? Umekuja kutuangamiza? Nakujua u nani. Wewe ni Mtakatifu
pekee wa Mungu!” 25 Yesu alimkemea pepo na kusema, “Nyamaza na utoke ndani
yake!” 26 Na roho mchafu alimwangusha chini na akatoka kwake wakati akilia
kwa sauti ya juu. 27 Na watu wote walishangaa, hivyo wakaulizana kila mmoja,
“Hii ni nini? Fundisho jipya lenye mamlaka? Hata huamuru pepo wachafu nao
wanamtii!” 28 Na habari kuhusu yeye mara moja zikasambaa kila mahali ndani ya
mkoa wote wa Galilaya. 29 Na mara moja baada ya kutoka nje ya sinagogi, waliingia
nyumbani mwa Simoni na Andrea wakiwa na Yakobo na Yohana. 30 Sasa mama
mkwe wa Simoni alikuwa amelala mgonjwa wa homa, na mara moja walimwambia
Yesu habari zake. 31 Hivyo alikuja, alimshika kwa mkono, na kumwinua juu; homa
ikaondoka kwake, na akaanza kuwahudumia. 32 Jioni hiyo wakati jua limekwisha
zama, walimletea kwake wote waliokuwa wagonjwa, au waliopagawa na pepo.
33 Mji wote walikusanyika pamoja katika mlango. 34 Aliwaponya wengi waliokuwa
wagonjwa wa magonjwa mbalimbali na kutoa pepo wengi, bali hakuruhusu pepo
kuongea kwa sababu walimjua. 35 Aliamka asubuhi na mapema, wakati ilikuwa

bado giza; aliondoka na kwenda mahali pa faragha na aliomba huko. 36 Simoni
na wote waliokuwa pamoja naye walimtafuta. 37 Walimpata na wakamwambia,
“Kila mmoja anakutafuta” 38 Aliwaambia, “Twendeni mahali pengine, nje katika
miji inayozunguka, ili niweze kuhubiri huko pia. Ndiyo sababu nilikuja hapa.”
39 Alikwenda akipita Galilaya yote, akihubiri katika masinagogi yao na kukemea
pepo. 40 Mwenye ukoma mmoja alikuja kwake. Alikuwa akimsihi; alipiga magoti
na alimwambia, “Kama unataka, waweza kunifanya niwe safi.” 41 Akisukumwa na
huruma, Yesu alinyosha mkono wake na kumgusa, akimwambia, “Ninataka. Uwe
msafi.” 42 Mara moja ukoma ukamtoka, na alifanywa kuwa safi. 43 Yesu akamwonya
vikali na akamwambia aende mara moja, 44 Alimwambia, “Hakikisha hausemi neno
kwa yeyote, lakini nenda, ujionyeshe kwa kuhani, na utoe dhabihu kwa ajili ya
utakaso ambayo Musa aliagiza, kama ushuhuda kwao.” 45 Lakini alikwenda na
kuanza kumwambia kila mmoja na kueneza neno zaidi hata Yesu hakuweza tena
kuingia mjini kwa uhuru. Hivyo alikaa mahali pa faragha na watu walikuja kwake
kutoka kila mahali.

# 2

1 Aliporudi Kaperinaumu baada ya siku chache, ilisikika kwamba alikuwa
nyumbani. 2 Watu wengi sana walikuwa wamekusanyika pale na haikuwepo nafasi
tena, hata ile ya pale mlangoni, na Yesu alisema neno kwao. 3 Kisha baadhi ya
watu walikuja kwake waliomleta mtu aliyekuwa amepooza; watu wanne walikuwa
wamembeba. 4 Wakati waliposhindwa kumkaribia kwa sababu ya umati wa watu,
waliondoa paa juu ya mahali pale alipokuwa. Na walipokuwa wamekwishatoboa
tundu, walishusha kitanda ambacho mtu aliyepooza alikuwa amelala. 5 Alipoiona
imani yao, Yesu alimwambia mtu aliyepooza, “mwanangu, dhambi zako zimesame-
hewa.” 6 Lakini baadhi ya waandishi wale waliokuwa wamekaa pale walijihoji
mioyoni mwao, 7 “Anawezaje mtu huyu kusema hivi? Anakufuru! Nani awezaye
kusamehe dhambi isipokuwa Mungu peke yake?” 8 Mara Yesu alijua rohoni mwake
walichokuwa wakififikiri miongoni mwao wenyewe. Aliwaambia, “Kwa nini mnafikiri
hivi mioyoni mwenu? 9 Lipi ni jepesi zaidi kusema kwa mtu aliyepooza, 'Dhambi
zako zimesamehewa' au kusema 'Simama, chukua kitanda chako, na utembee?'
10 Lakini ili wapate kujua ya kuwa Mwana wa Adamu ana mamlaka ya kusamehe
dhambi katika dunia, alimwambia yule aliyepooza, 11 “Nakuambia wewe, inuka,
chukua mkeka wako, na uende nyumbani kwako.” 12 Alisimama na mara moja
akachukua mkeka wake, na alikwenda nje ya nyumba mbele ya kila mtu, hivyo
wote walishangaa na walimpa Mungu utukufu, na wakasema “Kamwe, hatujawahi
kuona jambo kama hili.” 13 Aliienda tena kando ya ziwa, na umati wote wa watu
walikuja kwake, na akawafundisha. 14 Alipokuwa akipita alimwona Lawi mwana
wa Alfayo ameketi kwenye sehemu ya kukusanyia kodi na akamwambia, “Nifuate.”
Alisimama na kumfuata. 15 Na wakati Yesu alipokuwa akipata chakula katika nyumba
ya Lawi, wakusanya kodi wengi na watu wenye dhambi walikuwa wakila na Yesu na
wanafunzi wake, kwa kuwa walikuwa wengi nao walimfuata. 16 Wakati waandishi,
ambao walikuwa Mafarisayo, walipoona kwamba Yesu alikuwa akila na watu wenye
dhambi na wakusanya kodi, waliwaambia wanafunzi wake, “Kwa nini anakula na
wakusanya kodi na watu wenye dhambi?” 17 Wakati Yesu aliposikia hivi aliwaambia,
“Watu walio na afya katika mwili hawamhitaji tabibu; ni watu wagonjwa pekee
ndio wanamhitaji. Sikuja kuwaita watu wenye haki, lakini watu wenye dhambi.”
18 Wanafunzi wa Yohana na Mafarisayo walikuwa wakifunga. Na baadhi ya watu
walikuja kwake na kumwambia, “Kwa nini wanafunzi wa Yohana na mafarisayo
hufunga, lakini wanafunzi wako hawafungi? 19 Yesu aliwaambia, “Je waliohudhuria

harusini wanaweza kufunga wakati bwana harusi bado akiwa pamoja nao? Kwa
vyovyote bwana harusi akiwa bado yuko pamoja nao hawawezi kufunga.” 20 Lakini
siku zitakuja wakati bwana harusi atakapoondolewa kwao, na katika siku hizo
wao watafunga. 21 Hakuna mtu ashonaye kipande kipya cha nguo kwenye vazi
kuukuu, vinginevyo kiraka kitabanduka kutoka katika hilo, kipya kubanduka kutoka
katika kikuukuu, na kutakuwepo mpasuko mbaya. 22 Hakuna mtu atiaye divai mpya
katika viriba vikuukuu, vinginevyo divai itavipasua viriba na vyote viwili divai na
viriba vitapotea. Badala yake, weka divai mpya katika viriba vipya.” 23 Katika
siku ya Sabato Yesu alipita kwenye baadhi ya mashamba, na wanafunzi wake
walianza kuchukua baadhi ya masuke ya ngano. 24 Na Mafarisayo walimwambia,
“Tazama, kwa nini wanafanya kitu ambacho ni kinyume cha sheria katika siku
ya Sabato?” 25 Aliwaambia, “Hamkusoma kile alichofanya Daudi alipokuwa katika
uhitaji na njaa—yeye pamoja na watu waliokuwa pamoja naye? 26 Jinsi alivyoenda
katika nyumba ya Mungu wakati Abiathari alipokuwa kuhani mkuu na akala
mkate uliowekwa mbele—ambao ilikuwa kinyume cha sheria kwa mtu yeyote kula
isipokuwa makuhani—na aliwapa hata baadhi ya wale waliokuwa pamoja naye?”
27 Yesu alisema, “Sabato ilifanywa kwa ajili ya mwanadamu, siyo mwanadamu kwa
ajili ya Sabato. 28 Kwa hiyo, Mwana wa Adamu ni Bwana, hata kwa Sabato.”

# 3

1 Na tena aliingia ndani ya sinagogi na mle palikuwa na mtu mwenye mkono
uliopooza. 2 Baadhi ya watu walikuwa wakimfuatilia kwa ukaribu kuona kama
atamponya siku ya Sabato ili kwamba wamshitaki. 3 Yesu alimwambia mtu mwenye
mkono uliopooza, “ Inuka na usimame katikati ya umati huu.” 4 Kisha akawaambia
watu, “Je ni halali kutenda tendo jema siku ya Sabato au kutenda yasiyo haki; kuokoa
maisha, au kuua?” Lakini walibaki kimya. 5 Akawaangalia kwa hasira, akihuzunika
kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao, na akamwambia yule mtu, “Nyoosha mkono
wako”. Akaunyoosha na Yesu akamponya mkono wake. 6 Mafarisayo wakaenda nje
na mara wakafanya njama pamoja na Maherode dhidi yake ili kumuua. 7 Kisha
Yesu, pamoja na wanafunzi wake, walienda baharini, na umati mkubwa wa watu
uliwafuata ukitokea Galilaya na Uyahudi 8 na kutoka Yerusalemu na kutoka Idumaya
na mbele ya Yorodani na jirani ya Tiro na Sidoni, umati mkubwa, uliposikia kila
kitu alichokuwa anakifanya, walikuja kwake. 9 Na aliwaambia wanafunzi wake
kuandaa mtubwi mdongo kwa ajili yake kwa sababu ya umati, ili kwamba wasije
wakamsonga. 10 Kwa kuwa aliponya wengi, ili kila mtu aliyekuwa na mateso
alikuwa na shauku ya kumfikia ili amguse. 11 Popote roho wachafu walipomwona,
walianguka chini mbele yake na kulia, na walisema, “Wewe ni Mwana wa Mungu”.
12 Aliwaamuru kwa msisitizo wasifanye ajulikane. 13 Alienda juu ya mlima, na
akawaita aliowataka, na wakaenda kwake. 14 Akawachagua kumi na wawili
(aliowaita mitume), ili kwamba wawe pamoja naye na aweze kuwatuma kuhubiri,
15 na kuwa na mamlaka ya kutoa mapepo. 16 Na akawachagua kumi na wawili:
Simoni, aliyempa jina la Petro, 17 Yakobo mwana wa Zebedayo, na Yohana ndugu
yake Yakobo, aliyepewa jina la Bonagesi, hao ni, wana wa ngurumo, 18 na Andrea,
Filipo, Bartholomayo, Mathayo, Tomaso, Yakobo mwana wa Alfayo, Thadayo, Simoni
Mkananayo, 19 na Yuda Iskariote, ambaye atamsaliti. 20 Kisha alienda nyumbani,
na umati wa watu wakaja pamoja tena, hata wasiweze kula hata mkate. 21 Familia
yake waliposikia habari hiyo, walienda kumkamata, kwani walisema, “ Amerukwa
na akili”. 22 Waandishi waliokuja kutoka Yerusalemu walisema, “ Amepagawa na
Beelzebuli,” na, “ Kwa mtawala wa mapepo anatoa mapepo”. 23 Yesu aliwaita kwake
na kusema nao kwa mifano, “ Jinsi gani Shetani aweza kumtoa Shetani? 24 Kama

ufalme ukigawanyika wenyewe, ufalme huo hauwezi kusimama. 25 Kama nyumba
ikigawanyika yenyewe, nyumba hiyo haiwezi kusimama. 26 Kama Shetani atainuka
kinyume chake mwenyewe na kugawanyika, hawezi kusimama, na atakuwa amefika
mwisho wake. 27 Lakini hakuna hata mmoja awezaye kuingia ndani ya nyumba ya
mtu mwenye nguvu na kuiba vitu vyake bila kumfunga mwenye nguvu kwanza,
na kisha kukusanya kilichomo nyumbani. 28 Kweli nawambieni, dhambi zote za
wana wa watu zitasamehewa, pamoja na kufuru ambazo wanatamka, 29 lakini yeyote
atakaye mkufuru Roho Mtakatifu hatasamehewa kamwe, bali ana hatia ya dhambi
ya milele". 30 Yesu alilisema hili kwa sababu walikuwa wakisema, "Ana roho chafu".
31 Kisha mama yake na ndugu zake walikuja na kusimama nje. Wakamtuma mtu,
kumwita. 32 Na umati wa watu uliokuwa umekaa karibu naye wakamwambia,
"mama yako na ndugu zako wako nje, na wanakutafuta wewe". 33 Aliwajibu,
"Ni nani mama yangu na ndugu zangu?" 34 Aliwaangalia waliokuwa wamekaa
wamemzunguka, na akasema, "Tazama, hawa ni mama zangu na ndugu zangu!
35 Yeyote afanyaye mapenzi ya Mungu, mtu huyo ni ndugu yangu, na dada yangu,
na mama yangu".

# 4

1 Tena alianza kufundisha kandokando ya bahari. Na umati mkubwa ulikusanyika
ukamzunguka, akaingia ndani ya mtumbwi baharini, na kukaa. Umati wote
walikuwa pembeni mwa bahari ufukweni. 2 Na akawafundisha mambo mengi
kwa mifano, na akasema kwao kwa mafundisho yake. 3 Sikilizeni, mpanzi alienda
kupanda. 4 Alipokuwa akipanda, baadhi ya mbegu zilianguka njiani, na ndege wakaja
wakazila. 5 Mbegu zingine zilianguka kwenye mwamba, ambako hapakuwa na
udongo mwingi. Mara zikanyauka, kwa sababu hazikuwa na udongo wakutosha.
6 Lakini jua lilipochomoza, zilinyauka, na kwa sababu hazikuwa na mzizi, zilikauka.
7 Mbegu ziingine zilianguka katikati ya miiba. Miiba ilikua na ikazisonga, na
hazikuzaa matunda yeyote. 8 Mbegu zingine zilianguka kwenye udongo mzuri na
zikazaa matunda wakati zikikua na kuongezeka, zingine zilizaa mara thelathini
zaidi, na zingine sitini, na zingine mia". 9 Na akasema, "Yeyote mwenye masikio
ya kusikia, na asikie!" 10 Yesu alipokuwa peke yake, wale waliokuwa karibu naye
na wale kumi na wawili walimuuliza kuhusu mifano. 11 Akasema kwao, "Kwenu
mmepewa siri za ufalme wa Mungu. Lakini kwa walio nje kila kitu ni mifano,
12 ili wakitazama, ndiyo hutazama, lakini hawaoni, na kwa hiyo wanaposikia ndiyo
husikia, lakini hawaelewi, amasivyo wangegeuka na Mungu angeliwasamehe." 13 Na
akasema kwao, "Je hamuelewi mfano huu? Mtawezaje kuelewa mifano mingine?.
14 Mpanzi alipanda neno. 15 Baadhi ni wale walioanguka pembeni mwa njia, mahali
neno lilipopandwa. Na walipolisikia, mara Shetani akaja na kulichukua neno ambalo
lilipandwa ndani yao. 16 Na baadhi ni wale waliopandwa juu ya mwamba, ambao,
wanapolisikia neno, kwa haraka wanalipokea kwa furaha. 17 Na hawana mizizi
yoyote ndani yao, lakini huvumilia kwa muda mfupi. Halafu tabu na masumbufu
vinapokuja kwa sababu ya neno, mara hujikwaa. 18 Na wengine ni wale waliopandwa
katika miiba. Wanalisikia neno, 19 lakini masumbufu ya dunia, udanganyifu wa
mali, na tamaa za mambo mengine, huwaingia na kulisonga neno, na linashindwa
kuzaa matunda. 20 Kisha kuna wale ambao wamepandwa kwenye udongo mzuri.
Wanalisikia neno na kulipokea na huzaa matunda: baadhi thelathini, na baadhi
sitini, na baadhi mia moja." 21 Yesu akawaambia, " Je huwa unaleta taa ndani ya
nyumba na kuiweka chini ya kikapu, au chini ya kitanda? Huileta ndani na kuiweka
juu ya kiango. 22 Kwa kuwa hakuna chochote kilichojificha ambacho hakitajulikana,
na hakuna siri ambayo haitawekwa wazi. 23 Akiwapo mwenye masikio ya kusikia,

na asikie!” 24 Akawaambia, “ Iweni makini kwa kile mnachokisikia, kwa kuwa
kipimo mpimacho, ndicho mtakachopimiwa, na itaongezwa kwenu. 25 Kwa sababu
yeye aliyenacho, atapokea zaidi, na yule asiyenacho, kutoka kwake vitachukuliwa
hata vile alivyonavyo.” 26 Na akasema, “Ufalme wa Mungu umefananishwa na mtu
aliyepanda mbegu katika udongo. 27 Alipolala usiku na kuamka asubuhi, na mbegu
zikachipuka na kukua, ingawa hajui ilivyotokea. 28 Dunia hutoa mbegu yenyewe;
kwanza majani, halafu maua, halafu mbegu zilizo komaa. 29 Na wakati mbegu
itakapokua imeiva mara hupeleka mundu, kwa sababu mavuno yamewadia.” 30 Na
akasema, “tuufananishe ufalme wa Mungu na kitu gani, au tutumie mfano gani
kuuelezea?. 31 Ni kama mbegu ya haradali, ambapo ilipopandwa ni ndogo sana
kuliko mbegu zote duniani. 32 Hata, wakati imepandwa, inakuana kuwa kubwa zaidi
ya mimea yote ya bustani, na inafanya matawi makubwa, hata ndege wa mbinguni
huweza kufanya viota vyao kwenye kivuli chake.” 33 Kwa mifano mingi alifundisha
na alisema neno kwao, kwa kadiri walivyoweza kuelewa, 34 na hakusema nao bila
mifano. Lakini wakati alipokuwa peke yake, akawaelezea kila kitu wanafunzi wake.
35 Katika siku hiyo, wakati wa jioni ulipowadia, akasema kwao, “Twendeni upande
wa pili”. 36 Hivyo wakauacha umati, wakamchukua Yesu, wakati huo tayari alikuwa
ndani ya mtumbwi. Mitumbwi mingine ilikuwa pamoja naye. 37 Na upepo mkali
wa dhoruba na mawimbi yalikuwa yakiingia ndani ya mtumbwi na mtumbwi tayali
ulikuwa umejaa. 38 Lakini Yesu mwenyewe alikuwa kwenye shetri, amelala kwenye
mto. Wakamwamsha, wakisema, “Mwalimu, haujali sisi tunakufa?” 39 Na akaamka,
akaukemea upepo na akaiambia bahari, “'Iwe shwari, amani”. Upepo ukakoma, na
kulikuwa na utulivu mkubwa. 40 Na akasema kwao, “Kwa nini mnaogopa? Je hamna
imani bado?” 41 Walijawa na hofu kubwa ndani yao na wakasemezana wao kwa wao,
“ Huyu ni nani tena, kwa sababu hata upepo na bahari vya mtii?”.

# 5

1 Walikuja mpaka upande mwingine wa bahari, katika mkoa wa Gerasi 2 Na ghafla
wakati Yesu alipokuwa akitoka nje ya mtumbwi, mtu mwenye roho chafu alikuja
kwake kutoka makaburini. 3 Mtu huyu aliishi makaburini. Hakuna aliyeweza
kumzuia zaidi, hakuna hata kwa minyororo. 4 Alikuwa amefungwa nyakati nyingi
kwa pingu na minyororo. Aliikata minyororo na pingu zake zilivunjwa. Hakuna hata
mmoja aliyekuwa na nguvu za kumshinda. 5 Usiku na mchana akiwa makaburini na
milimani, alilia na kujikata yeye mwenyewe kwa mawe makali. 6 Alipomwona Yesu
kwa mbali, alikimbilia kwake na kuinama mbele yake. 7 Alilia kwa sauti kuu, “Wataka
nikufanyie nini, Yesu, Mwana wa Mungu aliye Juu sana? Ninakusihi kwa Mungu
mwenyewe, usinitese.” 8 Kwa kuwa alikuwa amemwambia, “Mtoke mtu huyu, wewe
roho mchafu.” 9 Naye alimwuliza, “Jina lako ni nani?” Naye alimjibu, “Jina langu ni
Legion, kwa kuwa tuko wengi.” 10 Alimsihi tena na tena asiwapeleke nje ya mkoa.
11 Sasa kundi kubwa la nguruwe lilikuwa likilishwa juu ya kilima, 12 nao walimsihi,
wakisema, “Tutume kwa nguruwe; tuingie ndani yao.” 13 Hivyo aliwaruhusu;
roho wachafu waliwatoka na kuingia ndani ya nguruwe, nao walikimbilia chini ya
kilima mpaka baharini, na karibia nguruwe elfu mbili walizama baharini. 14 Na
wale waliokuwa wakiwalisha nguruwe walikimbia na kutoa taarifa ya kilichotokea
katika mji na katika nchi. Ndipo watu wengi walitoka kwenda kuona kilichotokea.
15 Ndipo walikuja kwa Yesu na walimwona mtu aliyepagawa na pepo—aliyekuwa na
Jeshi—amekaa chini, amevikwa, na akiwa katika akili yake timamu, nao waliogopa.
16 Wale waliokuwa wameona kilichotokea kwa mtu aliyekuwa amepagawa na pepo
waliwaambia kilichotokea kwake na pia kuhusu nguruwe. 17 Nao walianza kumsihi
aondoke katika mkoa wao. 18 Na alipokuwa akiingia ndani ya mtumbwi, mtu

aliyekuwa amepagawa na mapepo alimsihi kwamba aende pamoja naye. 19 Lakini
hakumruhusu, lakini alimwambia, “Nenda nyumbani kwako na kwa watu wako, na
uwaambie alikufanyia Bwana, na rehema aliyokupa.” 20 Hivyo aliendа na alianza
kutangaza mambo makuu ambayo Yesu amefanya kwake katika Dekapoli, na kila
mmoja alistaajabu. 21 Na wakati Yesu alipovuka tena upande mwingine, ndani ya
mtumbwi, umati mkubwa ulikusanyika kumzunguka, alipokuwa kando ya bahari.
22 Na mmoja wa kiongozi wa sinagogi, aliyeitwa Yairo, alikuja, na alipomwona,
alianguka miguuni pake. 23 Akamsihi zaidi na zaidi, akisema, “ Binti yangu mdogo
anakaribia kufa. Ninakusihi, njoo na uweke mikono yako juu yake ili kwamba
aweze kupata afya na kuishi.” 24 Hivyo alikwenda pamoja naye, na umati mkubwa
ulimfuata nao walimzonga karibu wakimzunguka. 25 Kulikuwa na mwanamke
ambaye damu yake ilikuwa imetoka kwa miaka kumi na miwili. 26 Aliteseka vya
kutosha chini ya matabibu wengi na alitumia kila kitu alichokuwa nacho. Hata hivyo
hakusaidika kwa chochote, lakini badala yake alizidi kuwa na hali mbaya. 27 Alisikia
habari kuhusu Yesu. Hivyo alikuja nyuma yake wakati alipokuwa akitembea ndani
ya umati, naye aliligusa vazi lake. 28 Kwa kuwa alisema, “Kama nikiyagusa mavazi
yake tu, nitakuwa mzima.” 29 Alipomgusa, kutokwa damu kulikoma, na alijisikia
katika mwili wake kwamba aliponywa kutoka kwenye mateso yake. 30 Na ghafla
Yesu aligundua ndani yake mwenyewe kwamba nguvu zimemtoka. Na aligeuka
huku na huku katika umati wa watu na kuuliza, “Ni nani aliyeligusa vazi langu?”
31 Wanafunzi wake walimwambia, “Unaona umati huu umekusonga ukikuzunguka,
nawe wasema, 'Ni nani aliyenigusa?'” 32 Lakini Yesu alitazama huku na huku kuona
ambaye aliyekuwa amefanya hili. 33 Mwanamke, akijua kilichotokea kwake, aliogopa
na kutetemeka. Alikuja na alianguka chini mbele yake na kumwambia ukweli
wote. 34 Alisema kwake, “Binti, imani yako imekufanya uwe mzima. Enenda kwa
amani na uponywe kutoka kwenye ugonjwa wako.” 35 Alipokuwa akizungumza,
baadhi ya watu walikuja kutoka kwa kiongozi wa Sinagogi, wakisema, “Binti yako
amekufa. Kwa nini kuendelea kumsumbua mwalimu?” 36 Lakini Yesu aliposikia
ambacho walikisema, alimwambia kiongozi wa Sinagogi, “Usiogope. Amini tu.”
37 Hakumruhusu yeyote kuongozana naye, isipokuwa Petro, Yakobo, na Yohana,
ndugu yake Yakobo. 38 Walikuja nyumbani kwa kiongozi wa Sinagogi naye aliona
vurugu, kulia kwingi na kuomboleza. 39 Alipoingia nyumbani, aliwaambia, “Kwa nini
mmesikitika na kwa nini mnalia? Mtoto hajafa bali amelala.” 40 Walimcheka, lakini
yeye, aliwatoa wote nje, alimchukua baba wa mtoto na mama na wale waliokuwa
pamoja naye, na aliingia ndani alimokuwa mtoto. 41 Aliuchukua mkono wa mtoto na
alimwambia, “Talitha koum,” ambayo ni kusema, “Binti mdogo, nakuambia, amka.”
42 Ghafla mtoto aliamka na kutembea (kwa kuwa alikuwa na umri wa miaka kumi
na miwili). Na ghafla walishikwa na mshangao mkubwa. 43 Aliwaamuru kwa nguvu
kwamba hakuna yeyote anapaswa kujua kuhusu hili. Na aliwaambia wampatie yule
binti chakula.

# 6

1 Na akaondoka hapo na kwenda mjini kwao, na wanafunzi wake wakamfuata.
2 Sabato ilipofika, alianza kufundisha katika Sinagogi. Watu wengi walimsikia na
wakashangazwa. Wakasema, “Amepata wapi mafundisho haya?” “Ni hekima gani
hii aliyopewa?” “Anatendaje miujiza hii kwa mikono yake?” 3 “Je huyu si yule
seremala, mwana wa Mariamu na ndugu yao kina Yakobo, Yose, Yuda na Simioni?
Je dada zake si wanaishi papa hapa pamoja nasi?” Na hawakufurahishwa na
Yesu. 4 Yesu akawaambia, “Nabii hakosi heshima, isipokuwa katika mji wake na
miongoni mwa ndugu zake na nyumbani mwake.” 5 Hakuweza kutenda miujiza

hapo, ila aliwawekea mikono wagonjwa wachache akawaponya. 6 Alishangazwa
sana kwa sababu ya kutokuamini kwao. Kisha alivitembelea vijiji vya jirani
akifundisha. 7 Aliwaita wale wanafunzi kumi na wawili akaanza kuwatuma wawili
wawili. Aliwapa mamlaka juu ya pepo wachafu, 8 na kuwaamuru wasichukue
chochote wanapokwenda isipokuwa fimbo tu. Wasichukue mkate, wala mkoba, wala
fedha kibindoni; 9 lakini wavae viatu, na siyo kanzu mbili. 10 Na akawaambia,
"Nyumba yoyote mtakayoingia, kaeni hapo mpaka mtakapoondoka. 11 Na mji wowote
usipowapokea wala kuwasikiliza, ondokeni kwao, kung'uteni mavumbi ya miguu
yenu, iwe ushuhuda kwao." 12 Nao wakaenda wakitangaza watu watubu na kuacha
dhambi zao. 13 Waliwafukuza pepo wengi, na waliwapaka mafuta wagonjwa na
wakaponywa. 14 Mfalme Herode aliposikia hayo, kwa kuwa jina la Yesu lilikuwa
limejulikana sana. Baadhi walisema, "Yohana mbatizaji amefufuka na kwa sababu
hiyo, hii nguvu ya miujiza inafanya kazi ndani yake." 15 Baadhi yao wakasema, "Huyu
ni Eliya," Bado wengine wakasema, "Huyu ni nabii, kama mmoja wa wale manabii
wa zamani." 16 Lakini Herode aliposikia haya akasema, "Yohana, niliyemkata kichwa
amefufuliwa." 17 Maana Herode mwenyewe aliagiza Yohana akamatwe na alimfunga
gerezani kwa sababu ya Herodia (mke wa kaka yake Filipo) kwa sababu yeye
alikuwa amemuoa. 18 Kwa maana Yohana alimwambia Herode, "Si halali kumuoa
mke wa kaka yako." 19 Lakini Herodia alianza kumchukia na alikuwa akitaka
kumuua, lakini hakuweza, 20 maana Herode alimwogopa Yohana; alijua kwamba ni
mwenye haki mtu mtakatifu, na alimwacha salama. Na alipoendelea kumsikiliza
alihuzunika sana, lakini alifurahi kumsikiliza. 21 Hata ilipofika wakati mwafaka
ikiwa imekaribia siku ya kuzaliwa Herode akawaandalia moafisa wake karamu,
na makamanda, na viongozi wa Galilaya. 22 Ndipo binti wa Herodia akaingia na
kucheza mbele yao, akamfurahisha Herode na wageni walioketi wakati wa chakula
cha jioni. Ndipo mfalme akamwambia binti, "Niombe chochote unachotaka nami
nitakupa." 23 Akamwapia na kusema, chochote utakachoniomba, nitakupa, hata
nusu ya ufalme wangu." 24 Akatoka nje akamuuliza mama yake, "Niombe nini?"
Akasema, "Kichwa cha Yohana Mbatizaji." 25 Na mara moja akaingia kwa mfalme
akaanza kusema, "Nataka unipatie ndani ya sahani, kichwa cha Yohana Mbatizaji."
26 Mfalme alisikitishwa sana, lakini kwa sababu ya kiapo chake na kwa ajili ya wageni,
hakuweza kumkatalia ombi lake. 27 Hivyo, mfalme akatuma askari kati ya walinzi
wake na kuwaagiza kwenda kumletea kichwa cha Yohana. Mlinzi alikwenda kumkata
kichwa akiwa kifungoni. 28 Akakileta kichwa chake kwenye sahani na kumpatia binti,
na binti akampa mama yake. 29 Na wanafunzi wake waliposikia hayo, walikwenda
kuuchukua mwili wake wakaenda kuuzika kaburini. 30 Na mitume, walikusanyika
pamoja mbele ya Yesu, wakamweleza yote waliyofanya na waliyoyafundisha. 31 Naye
akawaambia, "Njooni wenyewe mahali pa faragha na tupumzike kwa muda."
Watu wengi walikuwa wanakuja na kuondoka, hata hawakupata nafasi ya kula.
32 Hivyo wakapanda mashua wakaenda mahali pa faragha peke yao. 33 Lakini
waliwaona wakiondoka na wengi wakawatambua, kwa pamoja walikimbia kwa
miguu kutoka miji yote, nao wakafika kabla yao. 34 Walipofika pwani, aliona
umati mkubwa na akawahurumia, kwa sababu walikuwa kama kondoo wasiokuwa
na mchungaji. Na akaanza kuwafundisha mambo mengi. 35 Muda ulipoendelea
sana, wanafunzi wakamjia wakamwambia,"Hapa ni mahali pa faragha na muda
umeendelea. 36 Uwaage waende miji ya jirani na vijiji ili wakajinunulie chakula."
37 Lakini akawajibu akisema, "Wapeni ninyi chakula." Wakamwambia, "Tunaweza
kwenda na kununua mikate yenye thamani ya dinari mia mbili na kuwapa
wale?" 38 Akawambia," Mna mikate mingapi? Nendeni mkaangalie." walipopata
wakamwambia, "Mikate mitano na samaki wawili." 39 Akawaamuru watu waketi

katika makundi juu ya majani mabichi. 40 Wakawaketisha katika makundi; makundi
ya mamia kwa hamsini. 41 Kisha akachukua mikate mitano na samaki wawili, na
kutazama mbinguni, akaibariki kisha akawapa wanafunzi waweke mbele ya umati.
Na kisha aligawa samaki wawili kwa watu wote. 42 Walikula wote hadi wakatosheka.
43 Walikusanya vipande vya mikate iliyobaki, Vikajaa vikapu kumi na viwili, na pia
vipande vya samaki. 44 Na walikuwa wanaume elfu tano waliokula mikate. 45 Mara
akawaambia wapande kwenye mashua waende sehemu nyingine, hadi Bethsaida,
wakati Yeye akiwaaga makutano. 46 Walipokuwa wamekwisha kuondoka, akaenda
mlimani kuomba. 47 Kulipokuwa jioni, na mashua yao wakati huo ikiwa katikati
ya bahari, naye alikuwa peke yake nchi kavu. 48 Na aliwaona wakitaabika kupiga
makasia kwa sababu upepo uliwazuia. Ilipokaribia asubuhi akawaendea, akitembea
juu ya maji, na alitaka kuwapita. 49 Lakini walipomwona anatembea juu ya maji,
wakaingiwa na wasiwasi wakidhani ni mzimu hata wakapiga kelele. 50 kwa sababu
walimwona wakajawa na hofu. Mara akasema nao akawaambia, “Muwe wajasiri! ni
mimi! Msiwe na hofu.” 51 Akaingia ndani ya mashua, na upepo ukaacha kuvuma, nao
wakamshangaa kabisa. 52 Hivyo hawakuwa wameelewa maana ya ile mikate. Maana
akili zao zilikuwa na uelewa mdogo. 53 Nao walipovuka ng'ambo, walifika nchi ya
Genesareti mashua ikatia nanga. 54 Walipotoka nje ya mashua, mara wakamtambua.
55 Wakakimbia kutangaza katika mkoa mzima na wakaanza kuwaleta wagonjwa kwa
machela, kila waliposikia anakuja. 56 Popote alipoingia katika vijiji, au mjini, au
katika nchi, waliwaweka wagonjwa mahali pa soko, na wakamsihi awaruhusu kugusa
pindo la vazi lake. Na wote waliomgusa waliponywa.

# 7

1 Mafarisayo na baadhi ya waandishi ambao walikuwa wametokea Yerusalemu
walikusanyika kumzunguka yeye. 2 Na waliona kuwa baadhi ya wanafunzi wake
walikula mkate kwa mikono najisi; ambayo haikuoshwa. 3 (kwa Mafarisayo na
Wayahudi wote hawali mpaka wameosha mikono yao vizuri; wanashikilia utamaduni
wa wazee. Wakati 4 Mafarisayo wanaporudi kutoka mahali pa soko, hawali
mpaka wameoga kwanza. Na kuna sheria zingine ambazo wanazifuata kabisa,
ikiwa ni pamoja na kuosha vikombe, masufuria, vyombo vya shaba, na hata viti
vinavyotumika wakati wa chakula.) 5 Mafarisayo na waandishi walimuuliza Yesu,
“ Kwa nini wanafunzi wako hawaishi kulingana na tamaduni za wazee, kwani
wanakula mkate pasipo kunawa mikono?” 6 Lakini yeye aliwaambia, “Isaya alitabiri
vizuri kuhusu ninyi wanafiki, aliandika, 'Watu hawa wananiheshimu kwa midomo
yao, lakini mioyo yao iko mbali na mimi. 7 Wananifanyia ibaada zisizo na maana,
wakifundisha sheria za wanadamu kama mapokeo yao.' 8 Mmeiacha sheria ya Mungu
na kushikilia kwa wepesi tamaduni za wanadamu.” 9 Na akasema kwao, “Mmeikataa
amri ya Mungu kwa urahisi ili kwamba mtunze tamaduni zenu! 10 Kwa kuwa Musa
alisema, 'mheshimu baba yako na mama yako,' na 'Yeye asemaye mabaya juu ya
baba yake au mama yake hakika atakufa.' 11 Lakini mnasema, 'kama mtu akisema
kwa baba yake au mama, “Msaada wowote ambao mngepokea kutoka kwangu ni
hazina ya Hekalu,”' (hiyo ni kusema kwamba, 'imetolewa kwa Mungu') 12 hivyo
haumruhusu kufanya jambo lolote kwa ajili ya baba au mama yake. 13 Mnaifanya
amri ya Mungu kuwa bure kwa kuleta tamaduni zenu. Na mambo mengi ya
jinsi hiyo mnayoyafanya.” 14 Aliwaita makutano tena na kuwaambia, “Mnisikilize
mimi, ninyi nyote, na mnielewe. 15 Hakuna chochote kutoka nje ya mtu ambacho
chaweza kumchafua mtu kiingiapo kwake. Bali ni kile kimtokacho mtu ndicho
kimchafuacho. 16 (Zingatia: mstari huu, “kama mtu yeyote ana masikio ya kusikia,
na asikie” haumo kwenye nakala za kale). 17 Yesu alipowaacha makutano na kuingia

nyumbani, wanafunzi wake wakamwuliza kuhusu mfano huo. [18] Yesu akasema,
“Na ninyi pia bado hamjaelewa? Hamuoni kwamba chochote kimuingiacho mtu
hakiwezi kumchafua, [19] kwa sababu hakiwezi kwenda kwenye moyo wake, lakini
kinaingia katika tumbo lake na kisha kinapita kwenda chooni.” Kwa maelezo haya
Yesu alivifanya vyakula vyote kuwa safi. [20] Alisema, “Ni kile ambacho kinamtoka
mtu ndicho kimchafuacho. [21] Kwa kuwa hutoka ndani ya mtu, nje ya moyo, hutoka
mawazo maovu, zinaa, wizi, mauaji, [22] uasherati, tamaa mbaya, uovu, udanganyifu,
kujamiiana, wivu, kashfa, majivuno, ujinga. [23] Maovu haya yote yanatoka ndani,
ndiyo yale yamchafuayo mtu.” [24] Aliamka kutoka pale na kuondoka kwenda katika
mkoa wa Tiro na Sidoni. Aliingia ndani na hakutaka mtu yeyote ajue kuwa alikuwa
hapo, lakini haikuwezekana kumficha. [25] Lakini ghafla mwanamke, ambaye mtoto
wake mdogo alikuwa na roho mchafu, alisikia habari zake, akaja, na akaanguka
miguuni pake. [26] Mwanamke huyo alikuwa Myunani, wa kabila la Kifoeniki. Alimsihi
yeye amfukuze pepo kutoka kwa binti yake. [27] Yesu akamwambia mwanamke,
“Waache watoto walishwe kwanza, kwa kuwa sio sawa kuuchukua mkate wa watoto
na kuwatupia mbwa.” [28] Lakini mwanamke akamjibu na kusema, “Ndiyo Bwana,
hata mbwa chini ya meza hula mabaki ya chakula cha watoto.” [29] Akamwambia,
“Kwa kuwa umesema hivi, uko huru kwenda. Pepo ameshamtoka binti yako.”
[30] Mwanamke alirudi nyumbani kwake na akamkuta binti yake amelala kitandani,
na pepo alikuwa amemtoka. [31] Yesu alitoka tena nje ya mkoa wa Tiro na kupitia
Sidoni kuelekea Bahari ya Galilaya mpaka kanda ya Dikapolisi. [32] Na wakamletea
mtu aliyekuwa kiziwi na alikuwa hawezi kuzungumza vizuri, walimsihi Yesu aweke
mikono juu yake. [33] Alimtoa nje ya kusanyiko kwa siri, na akaweka vidole vyake
kwenye masikio yake, na baada ya kutema mate, aligusa ulimi wake. [34] Alitazama
juu mbinguni, akahema na kumwambia, “Efata,” hiyo ni kusema “funguka!” [35] Na
muda ule ule masikio yakafunguka, na kilichokuwa kimezuia ulimi kiliharibiwa
na akaweza kuongea vizuri. [36] Na aliwaamuru wasimwambie mtu yeyote. Lakini
kadri alivyowaamuru, ndivyo walivyotangaza habari hizo kwa wingi. [37] Hakika
walishangazwa, na kusema, “Amefanya kila kitu vizuri. Hata amewafanya viziwi
kusikia na mabubu kuongea.”

# 8

[1] Katika siku hizo, kulikuwa tena na umati mkubwa, na hawakuwa na chakula.
Yesu akawaita wanafunzi wake akawaambia, [2] “Ninauhurumia umati huu, wameen-
delea kuwa nami kwa siku tatu na hawana chakula. [3] Nikiwatawanya warudi
majumbani kwao bila kula wanaweza wakazimia njiani kwa njaa. Na baadhi yao
wametoka mbali sana.” [4] Wanafunzi wake wakamjibu, “Tutapata wapi mikate ya
kutosha kuwashibisha watu hawa katika eneo hili lililoachwa?” [5] Akawauliza, “mna
vipande vingapi vya mikate?” Wakasema, “Saba”. [6] Aliuamuru umati ukae chini.
Akachukua mikate saba, akamshukuru Mungu, na kuivunja. Akawapa wanafunzi
wake waiweke mbele yao, nao wakaiweka mbele ya umati. [7] Pia walikuwa na samaki
wadogo wachache, na baada ya kushukuru, aliwaamuru wanafunzi wake wawagawie
hivi pia. [8] Walikula na wakatosheka. Na walikusanya vipande vilivyo baki, vikapu
vikubwa saba. [9] Walikaribia watu elfu nne. Na aliwaacha waende. [10] Mara aliingia
kwenye mashua na wanafunzi wake, na wakaenda katika ukanda ya Dalmanuta.
[11] Kisha Mafarisayo walitoka nje na kuanza kubishana naye. Walitaka awape ishara
kutoka mbinguni, kwa kumjaribu. [12] Akatafakari kwa kina moyoni mwake akasema,
“Kwa nini kizazi hiki kinatafuta ishara? Nawaambia ninyi kweli, hakuna ishara
itakayotolewa kwa kizazi hiki.” [13] Kisha akawaacha, akaingia ndani ya mashua
tena, akaondoka kuelekea upande mwingine. [14] Wakati huo wanafunzi walisahau

kuchukua mikate. Hawakuwa na mikate zaidi ya kipande kimoja kilichokuwa
kwenye mashua. 15 Aliwaonya na kusema, “Muwe macho na mjilinde dhidi ya chachu
ya Mafarisayo na chachu ya Herode. 16 Wanafunzi wakasemezana wao kwa wao,
“Ni kwa sababu hatuna mikate.” 17 Yesu alilitambua hili, na akawaambia, “Kwa
nini mnasemezana kuhusu kutokuwa na mikate? Hamjajua bado? Hamuelewi?
Mioyo yenu imekuwa miepesi? 18 Mna macho, hamuoni? Mna masikio, hamsikii?
Hamkumbuki? 19 Nilipoigawanya mikate mitano kwa watu elfu tano, mlichukua
vikapu vingapi vilivyo jaa vipande vya mikate?” Wakamjibu, “kumi na mbili.”
20 “Na nilipoigawanya mikate saba kwa watu elfu nne, mlichukua vikapu vingapi?”
21 Wakasema, “Saba.” Akawaambia, “Bado hamuelewi?” 22 Wakaja Bethsaida. Watu
hao walimleta kwa Yesu mtu kipofu na wakamsihi Yesu amguse. 23 Yesu akamshika
kwa mkono yule kipofu, na kumwongoza nje ya kijiji. Alipotema mate juu ya
macho yake na kunyosha mikono yake juu yake, alimuuliza, “Unaona chochote?”
24 Alitazama juu na kusema, “Naona watu wanaonekana kama miti inatembea.”
25 Ndipo akanyosha tena mikono yake juu ya macho yake, mtu yule akafungua macho
yake, aliona tena, na akaona kila kitu vizuri. 26 Yesu alimwacha aende nyumbani
na akamwambia, “Usiingie mjini.” 27 Yesu aliondoka na wanafunzi wake kwenda
vijiji vya Kaiseria ya Filipi. Wakiwa njiani aliwauliza wanafunzi, “Watu wanasema
mimi ni nani?” 28 Wakamjibu wakasema, “Yohana mbatizaji. Wengine wanasema,
'Eliya' na wengine, 'Mmoja wa Manabii.” 29 Akawauliza, “Lakini ninyi mnasema mimi
ni nani?” Petro kamwambia, “Wewe ni Kristo.” 30 Yesu akawaonya wasimwabie
mtu yeyote kumuhusu Yeye. 31 Na akaanza kuwafundisha ya kuwa Mwana wa
Adamu lazima ateseke kwa mambo mengi, na atakataliwa na viongozi na makuhani
wakuu, na waandishi, na atauawa, na baada ya siku tatu atafufuka. 32 Alisema haya
kwa uwazi. Ndipo Petro akamchukua pembeni na akaanza kumkemea. 33 Lakini
Yesu aligeuka na kuwatazama wanafunzi wake na akamkemea Petro na kusema,
“Pita nyuma yangu Shetani! Hujali mambo ya Mungu, isipokuwa mambo ya watu.”
34 Kisha akauita umati na wanafunzi wake pamoja, na kuwaambia, “Kama kuna mtu
anataka kunifuata, ajikane mwenyewe, achukue msalaba wake, na anifuate. 35 Kwa
kuwa yeyote anayetaka kuyaokoa maisha yake atayapoteza, na yeyote atakayepoteza
maisha yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya injili, atayaokoa. 36 Inamfaidia nini mtu,
kupata ulimwengu wote, na kisha kupata hasara ya maisha yake? 37 Mtu anaweza
kutoa nini badala ya maisha yake? 38 Yeyote anioneaye aibu na maneno yangu katika
kizazi hiki cha wazinzi na kizazi cha wenye dhambi, Mwana wa Adamu atamwonea
aibu atakapokuja katika ufalme wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu.

# 9

1 Na alisema kwao, “Hakika nasema kwenu, baadhi yenu kuna watu waliosimama
hapa hawataonja mauti kabla ya kuuona ufalme wa Mungu ukija kwa nguvu.”
2 Na baada ya siku sita, Yesu aliwachukua Petro, Yakobo na Yohana pamoja naye
mlimani, pekee yao. Ndipo alianza kubadilika mbele yao. 3 Mavazi yake yakaanza
kung'aa sana, meupe zaidi, meupe kuliko mng'arishaji yeyote duniani. 4 Ndipo
Eliya pamoja na Musa walitokea mbele yao, na walikuwa wakiongea na Yesu.
5 Petro alijibu akamwambia Yesu, “Mwalimu, ni vyema sisi kuwa hapa, na tujenge
vibanda vitatu, kimoja kwa ajili yako, kimoja kwa ajili Musa na kingine kwa ajili ya
Eliya.” 6 (Kwa kuwa hakujua nini cha kusema, waliogopa sana.) 7 Wingu lilitokea
na kuwafunika. Ndipo sauti ikatoka mawinguni ikisema, “ Huyu ni mwanangu
mpendwa. Msikieni yeye.” 8 Ghafla, walipokuwa wakitazama, hawakumuona
yeyote pamoja nao, isipokuwa Yesu tu. 9 Walipokuwa wanateremka kutoka mlimani,
aliwaamuru kutokumwambia mtu yeyote yale yote waliyoyaona, mpaka Mwana

wa Adamu atakapofufuka kutoka kwa wafu. [10] Ndipo waliyatunza mambo wao
wenyewe. Lakini walijadiliana wao kwa wao ni nini maana yake “kufufuliwa
kutoka kwa wafu” [11] Walimwuliza Yesu,”Kwa nini waandishi husema lazima Eliya aje
kwanza?” [12] Akawaambia, “hakika Eliya atakuja kwanza kuokoa vitu vyote. Kwa nini
imeandikwa Mwana wa Adamu lazima apate mateso mengi na achukiwe? [13] Lakini
nasema kwenu Eliya alikwisha kuja, na walimfanya kama walivyopenda, kama vile
maandiko yasemavyo kuhusu yeye.” [14] Na waliporudi kwa wanafunzi, waliona kundi
kubwa limewazunguka na Masadukayo walikuwa wanabishana nao. [15] Na mara
walipomwona, kundi lote lilishangaa na kumkimbilia kumsalimia. [16] Aliwauliza
wanafunzi wake, “Mnabishana nao juu ya nini?” [17] Mmoja wao katika kundi alimjibu,
“Mwalimu, nilimleta mwanangu kwako; ana roho chafu ambayo humfanya asiweze
kuongea, [18] na humsababishia kutetemeka na kumwangusha chini, na kutoka povu
mdomoni na kusaga meno na kukakamaa. Niliwaomba wanafunzi wako kumtoa
pepo, lakini hawakuweza. [19] Aliwajibu, “Kizazi kisichoamini, nitakaa nanyi kwa
muda gani? Nitachukuliana nanyi hadi lini? Mleteni kwangu.” [20] Walimleta mtoto
wake. Roho mchafu alipomwona Yesu, ghafla ilimtia katika kutetemeka. Mvulana
alianguka chini na kutoa povu mdomoni. [21] Yesu alimwuliza baba yake, “Amekuwa
katika hali hii kwa muda gani?” Baba alisema, “ Tangu utoto. [22] Mara nyingine
huanguka katika moto au kwenye maji, na kujaribu kumwangamiza. Kama unaweza
kufanya chochote tuhurumie na utusaidie.” [23] Yesu alimwambia, “Kama uko tayari?
Kila kitu kinawezekana kwa yeyote aaminiye.” [24] Ghafla baba wa mtoto alilia
na kusema, “ Naamini! Nisaidie kutokuamini kwangu.” [25] Wakati Yesu alipoona
kundi linakimbilia kwao, alimkemea roho mchafu na kusema, “wewe roho bubu
na kiziwi, nakuamuru mwache, usiingie kwake tena.” [26] Alilia kwa nguvu na
kumhangaisha mtoto na roho alimtoka. Mtoto alionekana kama amekufa, Ndipo
wengi walisema, “Amekufa,” [27] Lakini Yesu alimchukua kwa mkono akamwinua, na
mtoto alisimama. [28] Wakati Yesu alipoingia ndani, wanafunzi wake walimwuliza
faragha, “Kwa nini hatukuweza kumtoa?” [29] Aliwaambia, “ kwa namna hii hatoki
isipokuwa kwa maombi.” [30] Walitoka pale na kupitia Galilaya. Hakutaka mtu
yeyote ajue walipo, [31] kwa kuwa alikuwa anafundisha wanafunzi wake. Aliwaambia,
“Mwana wa Adamu atafikishwa mikononi mwa watu, na watamuua. Atakapokuwa
amekufa, baada ya siku tatu atafufuka tena.” [32] Lakini hawakuelewa maelezo
haya, na waliogopa kumwuliza. [33] Ndipo walifika Karperinaumu. Wakati akiwa
ndani ya nyumba aliwauliza, ''Mlikuwa mnajadili nini njiani”? [34] Lakini walikuwa
kimya. Kwani walikuwa wanabishana njiani kwamba nani alikuwa mkubwa
zaidi. [35] Alikaa chini akawaita kumi na wawili pamoja, na alisema nao, “Kama
yeyote anataka kuwa wa kwanza, ni lazima awe wa mwisho na mtumishi wa
wote.” [36] Alimchukua mtoto mdogo akamweka katikati yao. Akamchukua katika
mikono yake, akasema, [37] “Yeyote ampokeaye mtoto kama huyu kwa jina langu,
pia amenipokea mimi, na ikiwa mtu amenipokea, hanipokei mimi tu, lakini pia
aliyenituma.” [38] Yohana alimwambia, “Mwalimu tulimwona mtu anatoa pepo kwa
jina lako na tukamzuia, kwa sababu hatufuati.” [39] Lakini Yesu alisema, “Msimzuie,
kwa kuwa hakuna atakayefanya kazi kubwa kwa jina langu na ndipo baadaye aseme
neno baya lolote juu yangu. [40] Yeyote asiyekuwa kinyume nasi yuko upande wetu.
[41] Yeyote atakayekupa kikombe cha maji ya kunywa kwa sababu uko na Kristo, kweli
nawaambia, hatapoteza thawabu yake. [42] Yeyote anayewakosesha hawa wadogo
waniaminio mimi, ingekuwa vyema kwake kufungiwa jiwe la kusagia shingoni na
kutupwa baharini. [43] Kama mkono wako ukikukosesha ukate. Ni heri kuingia katika
uzima bila mkono kuliko kuingia kwenye hukumu ukiwa na mikono yote. Katika
moto “usiozimika”. [44] (Zingatia: Mstari hii, “Mahali ambapo funza hawafi na moto

usiozimika." haumo katika nakala za kale). 45 Kama mguu wako ukikukosesha, ukate.
Ni vyema kwako kuingia uzimani ukiwa kilema, kuliko kutupwa hukumuni na miguu
miwili. 46 (Zingatia: Mstari huu, "Mahali ambapo funza hawafi na moto usioweza
kuzimika" haumo kwenye nakala za kale). 47 Kama jicho lako likikukosesha ling'oe.
Ni vyema kwako kuingia katika Ufalme wa Mungu ukiwa na jicho moja, kuliko kuwa
na macho mawili na kutupwa kuzimu. 48 Mahali palipo na funza wasiokufa, na moto
usiozimika. 49 Kwa kuwa kila mmoja atakolezwa na moto. 50 Chumvi ni nzuri, kama
chumvi ikipoteza ladha yake, utaifanyaje iwe na ladha yake tena? Muwe na chumvi
miongoni mwenu wenyewe, na muwe na amani kwa kila mmoja."

# 10

1 Yesu aliondoka eneo hilo na akaenda katika mkoa wa Uyahudi na eneo la mbele ya
Mto Yorodani, na makutano walimfuata tena. Aliwafundisha tena, kama ilivyokuwa
kawaida yake kufanya. 2 Na Mafarisayo walikuja kumjaribu na wakamuuliza,
"Ni halali kwa mwanamume kuachana na mke wake?" 3 Yesu akawajibu, "Musa
aliwaamuru nini?" 4 Wakasema, "Musa aliruhusu kuandika cheti cha kuachana
na kisha kumfukuza mwanamke." 5 "Ni kwa sababu ya mioyo yenu migumu
ndiyo maana aliwaandikia sheria hii," Yesu aliwaambia. 6 "Lakini kutoka mwanzo
wa uumbaji, 'Mungu aliwaumba mwanamume na mwanamke.' 7 Kwa sababu hii
mwanamume atamwacha baba yake na mama yake na ataungana na mke wake, 8 na
hao wawili watakuwa mwili mmoja; Kwa kuwa si wawili tena, bali mwili mmoja.
9 Kwa hiyo alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe." 10 Walipokuwa
ndani ya nyumba, wanafunzi wake wakamwuliza tena kuhusu hili. 11 Akawaambia,
"Yeyote amwachaye mke wake na kumwoa mwanamke mwingine, anafanya uzinzi
dhidi yake. 12 Mwanamke naye akimwacha mme wake na kuolewa na mwanamme
mwingine, anafanya uzinzi." 13 Nao walimletea watoto wao wadogo ili awaguse,
lakini wanafunzi wakawakemea. 14 Lakini Yesu alipotambua hilo, hakufurahishwa
nalo kabisa akawaambia, "Waruhusuni watoto wadogo waje kwangu, na msiwazuie,
kwa sababu walio kama hawa ufalme wa Mungu ni wao. 15 Ukweli nawaambia,
yeyote asiyeupokea ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hakika hawezi kuingia
katika ufalme wa Mungu. 16 Kisha akawachukua watoto mikononi mwake na
akawabariki akiwawekea mikono yake juu yao. 17 Na alipoanza safari yake mtu
mmoja alimkimbilia na akapiga magoti mbele yake, akamwuliza, "Mwalimu Mwema,
nifanye nini ili niweze kurithi uzima ya milele?" 18 Na Yesu akasema, "Kwa nini
unaniita mwema? Hakuna aliye mwema, isipokuwa Mungu peke yake. 19 Unazijua
amri: 'Usiue, usizini, usiibe, usishuhudie uongo, usidanganye, mheshimu baba na
mama yako'." 20 Mtu yule akasema, "Mwalimu, haya yote nimeyatii tangu nikiwa
kijana." 21 Yesu alimwangalia na kumpenda. Akawambia, "Unapungukiwa kitu
kimoja. Unapaswa kuuza vyote ulivyo navyo na uwape masikini, na utakuwa na
hazina mbinguni. Ndipo uje unifuate." 22 Lakini alikata tamaa kwa sababu ya
maelezo haya; aliondoka akiwa mwenye huzuni, kwa kuwa alikuwa na mali nyingi.
23 Yesu akatazama pande zote na kuwaambia wanafunzi wake, "Ni jinsi gani ilivyo
vigumu kwa tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu! 24 Wanafunzi walishangazwa
kwa maneno haya. Lakini Yesu akawaambia tena, "Watoto, ni jinsi gani ilivyo vigumu
kuingia katika ufalme wa Mungu! 25 Ni rahisi kwa ngamia kupita kwenye tundu
la sindano, kuliko mtu tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu." 26 Walishangazwa
sana na wakasemezana, "Hivyo nani ataokoka" 27 Yesu akawaangalia na kusema,
" Kwa binadamu haiwezekani, lakini sio kwa Mungu. Kwa kuwa katika Mungu
yote yanawezekana." 28 "Petro akaanza kuzungumza naye, "Angalia tumeacha vyote
na tumekufuata." 29 Yesu akasema, "Ukweli nawaambia ninyi, hakuna aliyeacha

nyumba, au kaka, au dada, au mama, au baba, au watoto, au ardhi, kwa ajili yangu,
na kwa ajili ya Injili, 30 ambaye hatapokea mara mia zaidi ya sasa hapa duniani:
nyumba, kaka, dada, mama, watoto, na ardhi, kwa mateso, na ulimwengu ujao, uzima
wa milele. 31 Lakini wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho na walio wa
mwisho watakuwa wa kwanza." 32 Walipokuwa njiani, kwenda Yerusalemu, Yesu
alikuwa amewatangulia mbele yao. Wanafunzi walishangaa, na wale waliokuwa
wanafuata nyuma waliogopa. Ndipo Yesu akawatoa pembeni tena wale kumi na
wawili na akaanza kuwaambia ambacho kitamtokea hivi karibuni: 33 "Tazama,
tunakwenda mpaka Yerusalemu, na Mwana wa Adamu atafikishwa kwa makuhani
wakuu na waandishi. Watamhukumu afe na watamtoa kwa watu wa Mataifa.
34 Watamdhihaki, watamtemea mate, watampiga fimbo, na watamwua. Lakini baada
ya siku tatu atafufuka." 35 Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, walikuja kwake na
kusema, "Mwalimu, tunakuhitaji utufanyie chochote tukuombacho." 36 Aliwaambia,
"Mnataka niwatendee nini?" 37 Wakasema, "Turuhusu tukae nawe katika utukufu
wako, mmoja katika mkono wako wa kuume na mwingine mkono wako wa kushoto."
38 Lakini Yesu aliwajibu, "Hamjui mnachoomba. Mnaweza kukinywea kikombe
ambacho nitakiywea au kustahimili ubatizo ambao nitabatizwa?" 39 Wakamwambia,
"Tunaweza" Yesu akawaambia, "Kikombe nitakachokinywea, mtakinywea. Na
ubatizo ambao kwao nimebatizwa, mtaustahimili. 40 Lakini atakayekaa mkono
wangu wa kuume au mkono wangu wa kushoto sio mimi wa kutoa, lakini ni kwa wale
ambao kwao imekwisha andaliwa." 41 Wale wanafunzi wengine kumi waliposikia
haya, wakaanza kuwakasirikia Yakobo na Yohana. 42 Yesu akawaita kwake na
kusema, "Mnajua kuwa wale wanaodhaniwa kuwa watawala wa watu wa Mataifa
huwatawala, na watu wao mashuhuri huwaonyesha mamlaka juu yao." 43 Lakini
haipaswi kuwa hivi kati yenu. Yeyote atakaye kuwa mkubwa kati yenu lazima
awatumikie, 44 na yeyote atakaye kuwa wa kwanza kati yenu ni lazima awe mtumwa
wa wote. 45 Kwa kuwa Mwana wa Adamu hakuja kutumikiwa bali kutumika,
na kuyatoa maisha yake kuwa fidia kwa wengi." 46 Wakaja Yeriko. Alipokuwa
akiondoka Yeriko na wanafunzi wake na kundi kubwa, mwana wa Timayo, Batimayo,
kipofu mwombaji, alikaa kando ya barabara. 47 Aliposikia kuwa ni Yesu Mnazareti,
alianza kupiga kelele na kusema, "Yesu, Mwana wa Daudi, nihurumie!" 48 Wengi
walimkemea yule kipofu, wakimwambia anyamaze. Lakini alilia kwa sauti zaidi,
"Mwana wa Daudi, nihurumie!" 49 Yesu alisimama na kuamuru aitwe. Walimwita
yule kipofu, wakisema, "Kuwa shujaa! Inuka! Yesu anakuita." 50 Akalitupa pembeni
koti lake, akakimbia zaidi, na kuja kwa Yesu. 51 Yesu akamjibu na kusema, "Unataka
nikufanyie nini?" Yule mwanaume kipofu akamjibu, "Mwalimu, ninataka kuona."
52 Yesu akamwambia, "Nenda. Imani yako imekuponya." Hapo hapo macho yake
yakaona; na akamfuata Yesu barabarani.

# 11

1 Wakati huo walipokuja Yerusalemu, walipokaribia Besthfage na Bethania, katika
Mlima wa Mizeituni, Yesu aliwatuma wawili miongoni mwa wanafunzi wake 2 na
aliwaambia, "Nendeni katika kijiji kinachokabiliana nasi. Mara mtakapoingia humo,
mtamkuta mwanapunda ambaye hajapandwa. Mfungueni na mmlete kwangu.
3 Na kama yeyote akiwaambia, 'Kwa nini mnafanya hivi'?, mnapaswa kusema,
'Bwana anamhitaji na mara atamrudisha hapa'." 4 Walikwenda na kumkuta
mwanapunda amefungwa nje mlangoni kwenye mtaa ulio wazi, nao walimfungua.
5 Na baadhi ya watu walikuwa wamesimama pale na waliwaambia, "Mnafanya
nini, kumfungua mwanapunda huyo?" 6 Waliwaambia kama Yesu alivyowaambia,
na watu wakawaacha waende. 7 Wanafunzi wawili walimleta mwanapunda kwa

Yesu na walitandika mavazi yao juu yake ili Yesu aweze kumpanda. [8] Watu wengi
wakatandika mavazi yao barabarani, na wengine wakatandika matawi waliyoyakata
kutoka mashambani. [9] Wale waliokwenda mbele yake na wale waliomfuata walipiga
kelele, “Hosana! Amebarikiwa anayekuja kwa jina la Bwana. [10] Ubarikiwe ufalme
unaokuja wa baba yetu Daudi! Hosana kwa aliye juu” [11] Ndipo Yesu aliingia
Yerusalemu na alikwenda hekaluni na alitazama kila kitu. Sasa, wakati ulikuwa
umeenda, alikwenda Bethania pamoja nao kumi na wawili. [12] Siku iliyofuata,
wakati walipokuwa wakirudi kutoka Bethania, alikuwa na njaa. [13] Na akaona mti
wa mtini uliokuwa na majani kwa mbali, alikwenda kutazama kama angeweza
kupata chochote juu yake. Na wakati alipokwenda kwa huo, hakupata chochote
isipokuwa majani, kwa kuwa haikuwa majira ya mtini. [14] Aliuambia, “Hakuna
yeyote atakayekula tunda kutoka kwako tena”. Na wanafunzi wake wakasikia.
[15] Walikuja Yerusalemu, naye aliingia hekaluni na kuanza kuwatoa nje wauzaji
na wanunuzi ndani ya hekalu. Alizipindua meza za wabadilishaji wa fedha na
viti vya wale waliokuwa wakiuza njiwa. [16] Hakumruhusu yeyote kubeba chochote
hekaluni kilichoweza kuuzwa. [17] Aliwafundisha na akasema, “Je haikuandikwa,
'nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote'? Lakini mmeifanya
pango la wanyang'anyi”. [18] Makuhani wakuu na waandishi walisikia alivyokuwa
amesema, nao walitafuta njia ya kumwua. Hata hivyo walimwogopa kwa sababu
umati ulishangazwa na mafundisho yake. [19] Na kila wakati jioni ilipofika, waliondoka
mjini. [20] Walipokuwa wakitembea asubuhi, waliuona mti wa mtini umekauka mpaka
kwenye mizizi yake. [21] Petro alikumbuka na kusema, “Rabi! Tazama, mti wa
mtini ulioulaani umekauka”. [22] Yesu aliwajibu, “Muwe na imani katika Mungu.
[23] Amini nawaambia kwamba kila auambiaye mlima huu, 'Ondoka, na ukajitupe
mwenyewe baharini, 'na kama hana mashaka moyoni mwake lakini anaamini
kwamba alichokisema kitatokea, hivyo ndivyo Mungu atakavyofanya. [24] Kwa hiyo
ninawaambia: kila kitu muombacho na kuuliza kwa ajili yake, aminini kwamba
mmepokea, navyo vitakuwa vyenu. [25] Wakati mnaposimama na kuomba, mnapaswa
kusamehe chochote mlichonacho dhidi ya yeyote, ili kwamba Baba yenu aliye
mbinguni awasamehe pia ninyi makosa yenu. [26] (Zingatia: Mstari huu, “Lakini
msiposamehe, wala Baba yenu aliye mbinguni hatasamehe dhambi zenu” haumo
kwenye nakala za kale). [27] Walikuja Yerusalemu tena. Na Yesu alipokuwa akitembea
hekaluni, makuhani wakuu, waandishi na wazee walikuja kwake. [28] Walimwambia,
“Kwa mamlaka gani unafanya mambo haya?” Na ni nani aliyekupa mamlaka
kuyafanya haya?” [29] Yesu aliwaambia, “Nitawauliza swali moja. Niambieni na mimi
nitawaambia kwa mamlaka gani ninayafanya mambo haya. [30] Je, ubatizo wa Yohana
ulitoka mbinguni au ulitoka kwa wanadamu? Nijibuni.” [31] Walijadiliana miongoni
mwao na kushindana na kusema, “Kama tukisema, 'Kutoka mbinguni,' atasema, 'Kwa
nini basi hamkumwamini?' [32] Lakini kama tukisema, 'Kutoka kwa wanadamu,'...”
Waliwaogopa watu, kwa kuwa wote walishikilia kwamba Yohana alikuwa Nabii.
[33] Ndipo walimjibu Yesu na kusema, “Hatujui. Ndipo Yesu akawaambia, “Wala mimi
sitawaambia ni kwa mamlaka gani nayafanya mambo haya.

# 12

[1] Kisha Yesu alianza kuwafundisha kwa mifano. Akasema, “Mtu alipanda shamba la
mizabibu, akalizungushia uzio, na akachimba shimo la kusindika mvinyo. Akajenga
mnara na kisha akalipangisha shamba la mizabibu kwa wakulima wa mizabibu.
Kisha alisafiri safari ya mbali. [2] Wakati ulipofika, alimtuma mtumishi kwa wakulima
wa mizabibu kupokea kutoka kwao baadhi ya matunda ya shamba la mizabibu.
[3] Lakini walimkamata, wakampiga, na wakamfukuza bila chochote. [4] Akamtuma

kwao mtumishi mwingine, wakamjeruhi kichwani na kumtendea mambo ya aibu.
5 Bado alimtuma mwingine, na huyu mmoja walimwua. Waliwatendea wengine
wengi mambo kama hayo hayo, wakiwapiga na wengine kuwaua. 6 Alikuwa bado
na mtu mmoja zaidi wa kumtuma, mwana mpendwa. Naye alikuwa wa mwisho
aliyetumwa kwao. Akisema, “Watamheshimu mwanangu”. 7 Lakini wapangaji
walisemezana wao kwa wao, “Huyu ndiye mrithi. Njoni, hebu na tumwue, na
urithi utakuwa wetu.” 8 Walimvamia, wakamuua na kumtupa nje ya shamba la
mizabibu. 9 Kwa hiyo, Je! Atafanya nini mmiliki wa shamba la mizabibu? Atakuja
na kuwaangamiza wakulima wa mizabibu na atalikabidhi shamba la mizabibu kwa
wengine. 10 Hamjapata kusoma andiko hili? “Jiwe ambalo wajenzi walilikataa,
limekuwa jiwe la pembeni. 11 Hili lilitoka kwa Bwana, na ni la ajabu machoni
petu.” 12 Walitafuta kumkamata Yesu, Lakini waliwaogopa makutano, kwani walijua
kuwa alikuwa amenena mfano huo dhidi yao. Hivyo walimwacha na wakaenda
zao. 13 Kisha wakawatuma baadhi ya mafarisayo na maherodia kwake ili kumtega
kwa maneno. 14 Walipofika, wakamwambia, “Mwalimu, tunajua kwamba hujali
maoni ya yeyote na huonyeshi upendeleo kati ya watu. Unafundisha njia ya Mungu
katika ukweli. Je! Ni haki kulipa kodi kwa Kaisari au la? Je! Twaweza kulipa
au la? 15 Lakini Yesu alijua unafiki wao na kuwaambia, “Kwa nini mnanijaribu?
Nipeni dinari niweze kuitazama.” 16 Wakaleta moja kwa Yesu, Akawaambia, “Je!
ni sura ya nani na maandishi yaliyopo hapa ni ya nani? Wakasema, “Ya Kaisari.”
17 Yesu akawaambia, “Mpeni Kaisari vitu vya Kaisari na Mungu vitu vya Mungu.”
Wakamstaajabia. 18 Kisha Masadukayo, wasemao hakuna ufufuo, walimwendea.
Wakamuwuliza, wakisema, 19 “Mwalimu, Musa alituandikia kuwa, 'Ikiwa ndugu ya
mtu akifa na kumwacha mke nyuma yake, lakini hakuacha mtoto, mtu atamchukua
mke wa ndugu yake, na kujipatia watoto kwa ajili ya ndugu yake.' 20 Kulikuwa na
ndugu saba, wa kwanza alitwaa mke na kisha akafa, hakuacha watoto. 21 Kisha wa
pili alimchukua naye akafa, hakuacha watoto. Na wa tatu hali kadhalika. 22 Na wa
saba alikufa bila kuacha watoto. Mwishowe na mwanamke pia akafa. 23 Wakati
wa ufufuo, watakapofufuka tena, Je! Atakuwa mke wa nani? Kwani wale ndugu
wote saba walikuwa waume wake.” 24 Yesu aliwaambia, “Je! Hii si sababu kuwa
mmepotoshwa, kwa sababu hamjui maandiko wala nguvu za Mungu?” 25 Wakati wa
kufufuka toka kwa wafu, hawataoa wala kuingia katika ndoa, bali watakuwa kama
malaika wa mbinguni. 26 Lakini, kuhusu wafu ambao wanafufuliwa, Je! Hamkusoma
kutoka katika kitabu cha Musa, katika habari za kichaka, jinsi Mungu alivyosema
na kumwambia, 'Mimi ni Mungu wa Abrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa
Yakobo?' 27 Yeye si Mungu wa wafu, bali wa walio hai. Ni dhahiri mmepotoka.”
28 Mmoja wa waandishi alikuja na kuyasikia mazungumzo yao; aliona kwamba Yesu
aliwajibu vema. Alimwuliza, “Je! ni amri ipi iliyo ya muhimu zaidi katika zote?”
29 Yesu alimjibu, “Iliyo ya muhimu ni hii, “Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu, Bwana
ni mmoja. 30 Lazima umpende Bwana Mungu wako, kwa moyo wako yote, kwa roho
yako yote, kwa akili yako yote, na kwa nguvu zako zote.' 31 Amri ya pili ni hii, 'Lazima
umpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.' Hakuna amri nyingine kuu
zaidi ya hizi.” 32 Mwandishi akasema, “Vema Mwalimu! Umesema kweli kwamba
Mungu ni mmoja, na kwamba hakuna mwingine zaidi yake. 33 Kumpenda yeye kwa
moyo wote, na kwa ufahamu wote na kwa nguvu zote, na kumpenda jirani kama
mwenyewe, ni muhimu mno kuliko matoleo na dhabihu za kuteketeza.” 34 Wakati
Yesu alipoona ametoa jibu la busara, alimwambia, “Wewe hauko mbali na ufalme
wa Mungu.” Baada ya hapo hakuna hata mmoja aliye thubutu kumwuliza Yesu
maswali yoyote. 35 Na Yesu alijibu, wakati alipokuwa akifundisha katika hekalu,
akasema, “Je! waandishi husemaje kuwa Kristo ni mwana wa Daudi? 36 Daudi

mwenyewe katika Roho Mtakatifu, alisema, 'Bwana alisema kwa Bwana wangu, keti
katika mkono wangu wa kuume, mpaka niwafanye maadui wako kuwa chini ya
miguu yako.' [37] Daudi mwenyewe humwita Kristo, 'Bwana' Je! ni mwana wa Daudi
kwa jinsi gani?" Na kusanyiko kuu lilimsikiliza kwa furaha. [38] Katika mafundisho
yake Yesu alisema, "Jihadharini na waandishi, wanaotamani kutembea na kanzu
ndefu na kusalimiwa kwenye masoko [39] na kuketi kwenye viti vya wakuu katika
masinagogi na katika sikukuu kwa maeneo ya wakuu. [40] Pia wanakula nyumba za
wajane na wanaomba maombi marefu ili watu wawaone. Hawa watu watapokea
hukumu iliyo kuu." [41] Kisha Yesu aliketi chini karibu na sanduku la sadaka ndani
ya eneo la hekalu; alikuwa akitazama watu waliokuwa wakitia pesa zao ndani ya
sanduku. Watu wengi matajiri waliweka kiasi kikubwa cha pesa. [42] Kisha mwanamke
mjane maskini alikuja na kutia vipande viwili, thamani ya senti. [43] Kisha akawaita
wanafunzi wake na kuwaambia, "Amini nawaambia, mwanamke huyu mjane ametia
kiasi kikubwa zaidi ya wote ambao wameshatoa katika sanduku la sadaka. [44] Kwani
wote wametoa kutokana na wingi wa mapato yao. Lakini mwanamke mjane huyu,
kutoka katika umaskini wake, katia pesa yote ambayo alipaswa kuitumia kwa maisha
yake."

# 13

[1] Yesu alipokuwa akitembea kutoka hekaluni, mmoja wa wanafunzi wake
akamwuliza, "Mwalimu, tazama mawe haya yakushangaza na majengo!"
[2] Akamwambia, Unaona majengo haya makubwa? Hakuna hata jiwe moja litakalo
salia juu ya jingine ambalo halitaangushwa chini". [3] Naye alipokuwa amekaa
juu ya Mlima wa Mizeituni nyuma ya hekalu, Petro, Yakobo, Yohana na Andrea
wakamwuliza kwa siri, [4] "Tuambie, mambo haya yatakuwa lini? Ni nini dalili ya
mambo haya kutokea?" [5] Yesu alianza kuwaambia, "Kuweni makini kwamba mtu
yoyote asiwapotoshe. [6] Wengi watakuja kwa jina langu wakisema, 'Mimi ndiye', na
watawapotosha wengi. [7] Mtakaposikia vita na tetesi za vita, msiogope; mambo haya
hayana budi kutokea, lakini mwisho bado. [8] Taifa litainuka kinyume na taifa jingine,
na ufalme kinyume na ufalme. Patakuwa na matetemeko sehemu mbalimbali, na
njaa. Huu ni mwanzo wa utungu. [9] Iweni macho. Watawapeleka hadi mabarazani,
na mtapingwa katika masinagogi. Mtasimamishwa mbele ya watawala na wafalme
kwa ajili yangu, kama ushuhuda kwao. [10] Lakini injili lazima kwanza ihubiriwe
kwa mataifa yote. [11] Watakapo wakamata na kuwakabidhi, msiogope kuhusu kile
mtakachosema. Ndani ya muda huo, mtapewa nini cha kusema; hamtakuwa ninyi
mtakaoongea, bali Roho Mtakatifu. [12] Ndugu atamshitaki ndugu kuuawa, baba na
mtoto wake. Watoto watasimama kinyume cha baba zao na kuwasababisha kuuawa.
[13] Mtachukiwa na kila mtu kwa sababu ya jina langu. Lakini atakayevumilia mpaka
mwisho, mtu huyo ataokoka. [14] Mtakapoona chukizo la uharibifu limesimama
pale lisipotakiwa kusimama (asomaye na afahamu), ndipo walioko ndani ya Yuda
wakimbilie milimani, [15] naye aliyeko juu ya nyumba asishuke chini ya nyumba,
au kuchukua chochote kilichoko nje, [16] na aliyeko shambani asirudi kuchukua vazi
lake. [17] Lakini ole wao wanawake wenye mimba na wanyonyeshao katika siku
hizo! [18] Ombeni kwamba isitokee wakati wa baridi. [19] Kwani patakuwa na mateso
makubwa, ambayo hayajawahi kutokea, tangu Mungu alipoumba ulimwengu, mpaka
sasa, hapana, wala haitatokea tena. [20] Mpaka Bwana atakapopunguza siku, hakuna
mwili utakaookoka, lakini kwa ajili ya wateule, atakaowachagua, atapunguza namba
za siku. [21] Wakati huo kama mtu yeyote atawaambia, Tazama, Kristo yuko hapa!' au
'Tazama, yuko pale!' msiamini. [22] Kwani Wakristo wa uongo na manabii wa uongo
watatokea na watatoa ishara na maajabu, ili kwamba, wawadanganye, yamkini hata

wateule. 23 Iweni macho! Nimekwisha wambia haya yote kabla ya wakati. 24 Lakini
baada ya mateso ya siku hizo, jua litatiwa giza, mwezi hautatoa mwanga wake,
25 nyota zitaanguka kutoka angani, na nguvu zilizoko mbinguni zitatikisika. 26 Ndipo
watakapomwona Mwana wa Adamu akija mawinguni kwa nguvu kubwa na utukufu.
27 Ndipo atatuma malaika zake na atawakusanya pamoja wateule wake kutoka pande
kuu nne za dunia, kutoka mwisho wa dunia mpaka mwisho wa mbingu. 28 Kwa
mtini jifunzeni. Kama tawi liwezavyo kutoa na kuweka haraka majani yake, ndipo
mtajua kwamba kiangazi kiko karibu. 29 Ndivyo ilivyo, mtakapoona mambo haya
yakitokea, jueni kwamba yuko karibu, na malango. 30 Kweli, nawambieni, hiki kizazi
hakitapita mbali kabla mambo haya hayajatokea. 31 Mbingu na nchi zitapita, lakini
maneno yangu hayatapita kamwe. 32 Lakini kuhusu siku hiyo au saa, hakuna ajuaye,
hata malaika wa mbinguni, wala Mwana, ila Baba. 33 Iweni macho, Tazama, kwa
sababu hamjui ni muda gani yatatokea. (Zingatia: Mstari huu, “Muwe waangalifu,
Tazameni na ombeni kwa sababu...” haumo kwenye nakala za kale). 34 Ni kama
mtu anayeenda safarini: akaacha nyumba yake, na kumweka mtumwa wake kuwa
mtawala wa nyumba, kila mmoja na kazi yake. Na kumwamuru mlinzi kukaa macho.
35 Kwa hiyo iweni macho! Kwani hamjui ni lini bwana wa nyumba atakaporudi
nyumbani, yawezekana ni jioni, usiku wa manane, wakati jogoo atakapowika,
au asubuhi. 36 Kama akija ghafla, asikukute umelala. 37 Kile nikisemacho kwako
nakisema kwa kila mtu: Kesheni”!

# 14

1 Ilikuwa siku mbili tu baada ya sikukuu ya Pasaka na ya Mikate Isiyotiwa Chachu.
Makuhani wakuu na waandishi walikuwa wakitafuta namna ya kumkamata Yesu
kwa hila na kumuua. 2 Kwa kuwa walisema, “Sio wakati huu wa sikukuu, watu
wasije wakafanya ghasia.” 3 Wakati Yesu alipokuwa Bethania nyumbani kwa Simoni
mkoma, na alipokuwa akielekea mezani, mwanamke mmoja alikuja kwake akiwa
na chupa ya marashi ya nardo safi yenye gharama kubwa sana, aliivunja chupa na
kuimimina juu ya kichwa chake. 4 Lakini kulikuwa na baadhi yao waliokasirika.
Waliambiana wao kwa wao wakisema, “Ni nini sababu ya upotevu huu? 5 Manukato
haya yangeweza kuuzwa kwa zaidi ya dinari mia tatu, na wakapewa maskini.” Nao
walimkemea. 6 Lakini Yesu alisema, “Mwacheni peke yake. Kwa nini mnamsumbua?
Amefanya jambo zuri kwangu. 7 Siku zote maskini mnao, na wakati wowote
mnapotamani mnaweza kufanya mazuri kwao, lakini hamtakuwa nami wakati
wote. 8 Amefanya kile anachoweza: ameupaka mwili wangu mafuta kwa ajili ya
maziko. 9 Kweli nawaambia, kila mahali injili inapohubiriwa katika ulimwengu
wote, kile alichofanya mwanamke huyu kitazungumzwa kwa ukumbusho wake.
10 Kisha Yuda Iskariote, mmoja wa wale kumi na wawili, alikwenda kwa wakuu
wa makuhani ili kwamba apate kumkabidhi kwao. 11 Wakati wakuu wa Makuhani
waliposikia hivyo, walifurahi na wakaahidi kumpa fedha. Alianza kutafuta nafasi
ya kumkabidhi kwao. 12 Katika siku ya kwanza ya mkate usiotiwa chachu, wakati
walipotoa mwanakondoo wa pasaka, wanafunzi wake walimwambia, “Unataka
twende wapi tukaandae ili upate kula mlo wa Pasaka?” 13 Aliwatuma wanafuzi
wake wawili na kuwaambia, “Nendeni mjini, na mwanamume ambaye amebeba
mtungi ataonana nanyi. Mfuateni. 14 Nyumba atakayoingia, mfuateni na mmwambie
mwenye nyumba hiyo, 'Mwalimu asema, “Kiko wapi chumba cha wageni mahali
nitakapokula Pasaka na wanafunzi wangu?” 15 Atawaonesha chumba cha juu
kikubwa chenye samani ambacho kiko tayari. Fanyeni maandalizi kwa ajili yetu
pale.” 16 Wanafunzi waliondoka wakaenda mjini; walikuta kila kitu kama alivyokuwa
amewaambia, na wakaandaa mlo wa Pasaka. 17 Wakati ilipokuwa jioni, alikuja na

wale Kumi na wawili. 18 Na walipokuwa wakiikaribia meza na kula, Yesu alisema,
“Kweli nawaambia, mmoja kati yenu anayekula pamoja nami atanisaliti.” 19 Wote
walisikitika, na mmoja baada ya mwingine walimwambia, “Hakika siyo mimi?”
20 Yesu alijibu na kuwaambia, “Ni mmoja wa Kumi na wawili kati yenu, mmoja
ambaye sasa anachovya tonge katika bakuli pamoja nami. 21 Kwa kuwa Mwana
wa Adamu atakwenda kama vile maandiko yasemavyo juu yake. Lakini ole wake
mtu yule ambaye kupitia yeye Mwana wa Adamu atasalitiwa! Ingekuwa vizuri zaidi
kwake kama mtu yule asingezaliwa.” 22 Na walipokuwa wakila, Yesu alichukua
mkate, akaubariki, na kuumega. Aliwapa akisema, “Chukueni. Huu ni mwili
wangu.” 23 Alichukua kikombe, akashukuru, na akawapatia, na wote wakakinywea.
24 Aliwaambia, “Hii ni damu yangu ya agano, damu imwagikayo kwa ajili ya wengi.
25 Kweli nawaambia, sitakunywa tena katika zao hili la mzabibu mpaka siku ile
nitakapokunywa mpya katika ufalme wa Mungu.” 26 Walipokwisha kuimba wimbo,
walikwenda nje katika Mlima wa Mizeituni. 27 Yesu aliwaaambia, “Ninyi nyote
mtajitenga mbali kwa sababu yangu, kwa kuwa imeandikwa, 'Nitampiga mchungaji
na kondoo watatawanyika.' 28 Lakini baada ya kufufuka kwangu, nitawatangulia
mbele yenu Galilaya.” 29 Petro alimwambia, “Hata kama wote watakuacha, mimi
sitakuacha.” 30 Yesu alimwambia, “Kweli nakuambia, usiku huu, kabla jogoo
hajawika mara mbili, utakuwa umenikana mara tatu.” 31 Lakini Petro alisema, “Hata
itanilazimu kufa pamoja nawe, sitakukana.” Wote walitoa ahadi ile ile. 32 Walikuja
kwenye eneo lililoitwa Gethsemane, na Yesu akawaambia wanafunzi wake, “Kaeni
hapa wakati nasali.” 33 Aliwachukua Petro, Yakobo, na Yohana pamoja naye, akaanza
kuhuzunika na kutaabika sana. 34 Aliwaambia, “Nafsi yangu ina huzuni sana,
hata kufa. Bakini hapa na mkeshe.” 35 Yesu alienda mbele kidogo, akaanguka
chini, akaomba, kama ingewezekana, kwamba saa hii ingemwepuka. 36 Alisema,
“Aba, Baba, Mambo yote kwako yanawezekana. Niondolee kikombe hiki. Lakini
siyo kwa mapenzi yangu, bali mapenzi yako.” 37 Alirudi na kuwakuta wamelala,
na akamwambia Petro, “Simoni, je umelala? Hukuweza kukesha hata saa moja?
38 Kesheni na muombe kwamba msije mkaingia katika majaribu. Hakika roho i
radhi, lakini mwili ni dhaifu.” 39 Alienda tena na kuomba, na alitumia maneno
yaleyale. 40 Alikuja tena akawakuta wamelala, kwa kuwa macho yao yalikuwa
mazito na hawakujua nini cha kumwambia. 41 Alikuja mara ya tatu na kuwaambia,
“Bado mmelala na kupumzika? Yatosha! Saa imefika. Tazama! Mwana wa Adamu
atasalitiwa mikononi mwa wenye dhambi. 42 Amkeni, twendeni. Tazama, yule
anayenisaliti yuko karibu.” 43 Mara tu alipokuwa bado anaongea, Yuda, mmoja wa
wale kumi na wawili, alifika, na kundi kubwa kutoka kwa wakuu wa makuhani,
waandishi na wazee wenye mapanga na marungu. 44 Wakati huo msaliti wake
alikuwa amewapa ishara, akisema, Yule nitakayembusu, ndiye. Mkamateni na
kumpeleka chini ya ulinzi.” 45 Wakati Yuda alipofika, moja kwa moja alienda kwa
Yesu na kusema, “Mwalimu!” Na akambusu. 46 Kisha wakumtia chini ya ulinzi na
kumkamata. 47 Lakini mmoja kati yao aliyesimama karibu naye alichomoa upanga
wake akampiga mtumishi wa kuhani mkuu na kumkata sikio. 48 Yesu aliwaambia,
“Mmekuja kunikamata kwa mapanga na marungu kama mnyang'anyi? 49 Wakati
kila siku nilikuwa nanyi na nikifundisha hekaluni, hamkunikamata. Lakini hili
limefanyika ili maandiko yatimie. 50 Na wale wote waliokuwa na Yesu walimwacha
na kukimbia. 51 Kijana mmoja alimfuata, aliyekuwa amevaa shuka tu aliyokuwa
amejifunika kumzunguka; walimkamata lakini 52 aliwaponyoka akaiacha shuka pale
akakimbia uchi. 53 Walimwongoza Yesu kwa kuhani mkuu. Pale walikusanyika
pamoja naye makuhani wakuu wote, wazee, na waandishi. 54 Petro naye alimfuata
Yesu kwa mbali, kuelekea kwenye ua wa kuhani mkuu. Aliketi pamoja na walinzi,

waliokuwa karibu na moto wakiota ili kupata joto. 55 Wakati huo makuhani wakuu
wote na Baraza lote walikuwa wakitafuta ushahidi dhidi ya Yesu ili wapate kumwua.
Lakini hawakuupata. 56 Kwa kuwa watu wengi walileta ushuhuda wa uongo dhidi
yake, lakini hata ushahidi wao haukufanana. 57 Baadhi walisimama na kuleta
ushahidi wa uongo dhidi yake; wakisema, 58 “Tulimsikia akisema, 'Nitaliharibu
hekalu hili lililotengenezwa kwa mikono, na ndani siku tatu nitajenga lingine
lisilotengenezwa kwa mikono.'” 59 Lakini hata ushahidi wao haukufanana. 60 Kuhani
mkuu alisimama katikati yao na akamwuliza Yesu, “Je, huna jibu? Watu hawa
wanashuhudia nini dhidi yako?” 61 Lakini alikaa kimya na hakujibu chochote. Mara
Kuhani mkuu alimwuliza tena, “Je wewe ni Kristo, mwana wa Mbarikiwa?” 62 Yesu
alisema, “Mimi ndiye. Na utamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kulia
wa nguvu akija na mawingu ya mbinguni.” 63 Kuhani mkuu alirarua mavazi yake
na kusema, “Je, bado tunahitaji mashahidi? 64 Mmesikia kufuru. Uamuzi wenu ni
upi?” Na wote walimhukumu kama mmoja aliyestahili kifo. 65 Baadhi wakaanza
kumtemea mate na kumfunika uso na kumpiga na kumwambia, “Tabiri!” Maafisa
walimchukua na kumpiga. 66 Na Petro alipokuwa bado yuko chini uani, mtumishi
mmoja wa wasichana wa kuhani mkuu alikuja kwake. 67 Alimwona Petro alipokuwa
amesimama akiota moto, na alimtazama kwa kumkaribia. Kisha alisema, “Nawe pia
ulikuwa na Mnazareti, Yesu”. 68 Lakini alikataa, akisema, “Sijui wala sielewi kuhusu
kile unachosema!” Kisha alitoka akaenda nje uani. (Zingatia; Mstari huu, “Na jogoo
akawika” haumo kwenye nakala za kale). 69 Lakini mtumishi wa kike pale, alimwona
na alianza kuwaambia tena wale ambao walikuwa wamesimama pale, “Mtu huyu ni
mmoja wao!” 70 Lakini alikana tena. Baadaye kidogo wale waliokuwa wamesimama
pale walikuwa wakimwambia Petro, “Hakika wewe ni mmoja wao, kwa maana wewe
pia ni Mgalilaya.” 71 Lakini alianza kujiweka mwenyewe chini ya laana na kuapa,
“Simjui mtu huyu mnayemsema.” 72 Kisha jogoo aliwika mara ya pili. Kisha Petro
alikumbuka maneno ambayo Yesu aliyokuwa amemwambia: “Kabla jogoo hajawika
mara mbili, utanikana mara tatu.” Na alianguka chini na kulia.

# 15

1 Asubuhi na mapema wakuu wa makuhani walikutana pamoja na wazee na waan-
dishi na baraza zima la wazee. Kisha wakamfunga Yesu wakampeleka kwa Pilato.
Pilato akamwuliza, “wewe ni Mfalme wa Wayahudi?” 2 “Akamjibu, “Wewe umesema
hivyo.” 3 Wakuu wa makuhani wakaeleza mashitaka mengi juu ya Yesu. 4 Pilato
akamwuliza tena, “Hujibu chochote? Huoni jinsi wanavyokushtaki kwa mambo
mengi? 5 Lakini Yesu hakumjibu Pilato, na hiyo ilimshangaza. 6 Kwa kawaida wakati
wa sikukuu humfungulia mfungwa mmoja, mfungwa waliyemwomba. 7 Kulikuwapo
wahalifu gerezani, miongoni mwa wauaji kati ya walioasi wanaotumikia makosa yao.
Alikuwepo mtu mmoja aitwaye Baraba. 8 Umati ulikuja kwa Pilato, na kumwomba
afanye kama alivyofanya huko nyuma. 9 Pilato akawajibu na kusema, “Mnataka
niwafungulie Mfalme wa Wayahudi?” 10 Kwa kuwa alijua ni kwa sababu ya wivu
wakuu wa makuhani walimkamata Yesu na kumleta kwake. 11 Lakini wakuu wa
makuhani walichochea umati kupiga kelele kwa sauti kwamba afunguliwe Baraba
badala yake. 12 Pilato akawajibu tena na kusema, “Nimfanye nini Mfalme wa
Wayahudi? 13 Wakapiga kelele tena, “Msulibishe!” 14 Pilato akasema, “Amefanya
jambo gani baya?” Lakini wakazidi kupiga kelele zaidi na zaidi “Msulibishe.” 15 Pilato
akitaka kuwaridhisha umati, akawafungulia Baraba. Akampiga Yesu mijeledi kisha
akamtoa ili asulibiwe. 16 Askari walimwongoza hadi ndani ya ua (ule ulio ndani
ya kambi) na walikusanyika pamoja kikosi cha askari. 17 Wakamvika Yesu kanzu
ya rangi ya zambarau, na wakasokota taji ya miiba wakamvika. 18 Wakaanza

kumdhihaki na kusema, “Salam, Mfalme wa Wayahudi!” 19 Wakampiga kichwani
kwa mwanzi na kumtemea mate. Wakapiga magoti mbele yake kwa kumheshimu.
20 Hata wakiisha kumdhihaki, wakamvua ile kanzu ya rangi ya zambarau na
kumvika mavazi yake, na wakamtoa nje kwenda kumsulibisha. 21 Wakamlazimisha
mpita njia kumsaidia, aliyekuwa anaingia mjini kutoka shamba. Aitwaye Simoni
Mkirene (baba yake Iskanda na Rufo); wakamlazimisha kubeba msalaba wa Yesu.
22 Askari wakampeleka Yesu mahali paitwapo Goligotha (maana ya tafsiri hii ni,
Sehemu ya Fuvu la kichwa). 23 Wakampa mvinyo iliyochanganywa na manemane,
lakini hakunywa. 24 Wakamsulibisha na wakagawana mavazi yake, wakayapigia
kura kuamua kipande atakachopata kila askari. 25 Yapata saa tatu asubuhi
walipomsulibisha. 26 Wakaweka juu yake ubao ulioandikwa shitaka, “Mfalme wa
Wayahudi.” 27 Walimsubisha pamoja na majambazi wawili, mmoja upande wake wa
kulia na mwingine kushoto kwake. 28 (Zingatia: Mstari huu, “Na maandiko yakatimia
yaliyonena” haumo katika nakala za kale). 29 Nao waliokuwa wakipita walimtukana,
wakitikisa vichwa vyao wakisema, “Aha! wewe utakayevunja hekalu na kulijenga
kwa siku tatu, 30 jiokoe mwenyewe na ushuke chini toka msalabani!” 31 Kwa namna
ile ile wakuu wa makuhani walimdhihaki wakisemezana, pamoja na waandishi na
kusema, “Aliwaokoa wengine, lakini hawezi kujiokoa mwenyewe. 32 Kristo Mfalme
wa Israel, shuka chini sasa toka msalabani, ili tuweze kuona na kuamini.” Na wale
waliosulubiwa pamoja naye pia walimdhihaki. 33 Ilipofika saa sita, giza likaja juu ya
nchi yote hadi saa tisa. 34 Wakati wa saa tisa, Yesu alipiga kelele kwa sauti kubwa,
“Eloi, Eloi, lama sabaktani?” ikiwa na maana “Mungu wangu, Mungu wangu, kwa
nini umeniacha?” 35 Baadhi ya hao waliosimama waliposikia wakasema, “Tazama,
anamwita Eliya.” 36 Mtu mmoja akakimbia, akajaza siki katika sponji na kuiweka juu
ya mti wa mwanzi, akampa ili anywe. Mtu mmoja akasema, “Ngoja tuone kama Eliya
atakuja kumshusha chini.” 37 Kisha Yesu akalia kwa sauti kubwa na akafa. 38 Pazia la
hekalu likagawanyika vipande viwili toka juu mpaka chini. 39 Ofisa mmoja aliyekuwa
amesimama akimwelekea Yesu, alipoona amekufa kwa jinsi ile, akasema, “Kweli
huyu mtu alikuwa Mwana wa Mungu.” 40 Walikuwepo pia wanawake waliokuwa
wakitazama kwa mbali. Miongoni mwao alikuwepo Mariamu Magdalena, Mariamu
(mama yake Yakobo mdogo wa Yose), na Salome. 41 Wakati alipokuwa Galilaya
walimfuata na kumtumikia. Na wanawake wengine wengi pia waliambatana naye
hadi Yerusalemu. 42 Kulipokuwa jioni, na kwa kuwa ilikuwa siku ya maandalio,
siku kabla ya Sabato, 43 Yusufu wa Arimathaya alikuja pale. Alikuwa ni mjumbe wa
Baraza anayeheshimiwa mtu anayeutarajia Ufalme wa Mungu. Kwa ujasiri akaenda
kwa Pilato, na kuuomba mwili wa Yesu. 44 Pilato akashangazwa kwamba Yesu tayari
amekufa; akamwita yule afisa akamwuliza kama Yesu amekufa. 45 Alipopata uhakika
kwa afisa kwamba amekufa, alimruhusu Yusufu kuuchukua mwili. 46 Yusufu alikuwa
amenunua sanda. Akamshusha toka msalabani, akamfunga kwa sanda, na kumweka
ndani ya kaburi lililochimbwa katika mwamba. Kisha akalivingirisha jiwe mlangoni
mwa kaburi. 47 Mariamu Magdalena na Mariamu mama yake Yose waliona sehemu
alipozikwa Yesu.

# 16

1 Wakati sabato ilipokwisha, Mariamu Magdalena na Mariamu mama yake na
Yakobo, na Salome, walinunua manukato mazuri, ili waweze kuja na kuupaka mafuta
mwili wa Yesu kwa ajili ya maziko. 2 Asubuhi na mapema siku ya kwanza ya
juma, walienda kwenye kaburi wakati jua lilipochomoza. 3 Wakisemezana wao
kwa wao, “Nani ataliviringisha jiwe kwa ajili yetu ili tuingie kaburini?” 4 Wakati
walipotazama, walimuona mtu amekwisha kulivingirisha jiwe, ambalo lilikuwa

kubwa sana. 5 Wakaingia kwenye kaburi na wakamwona kijana amevaa joho
jeupe, ameketi upande wa kulia, na wakashangazwa. 6 Akawaambia, “Msiogope.
Mnamtafuta Yesu, wa Nazareti, aliyesulibiwa. Amefufuka! Hayupo hapa. Tazama
mahali pale walipokuwa wamemweka. 7 Nendeni, mkawaambie wanafunzi wake na
Petro ya kuwa amewatangulia kuelekea Galilaya. Huko mtamwona, kama alivyokua
amewaambia.” 8 Wakaondoka na kukimbia kutoka kwenye kaburi; walitetemeka
na walishangazwa. Hawakusema chochote kwa mtu yeyote sababu waliogopa sana.
9 (Zingatia: Nakala za kale hazina Marko 16: 9-20) Mapema katika siku ya kwanza
ya juma, baada ya kufufuka, alimtokea kwanza Mariamu Magdalena, ambaye kutoka
kwake alimtoa mapepo saba. 10 Aliondoka na kuwaambia wale ambao walikuwa
pamoja naye, wakati walipokuwa wakihuzunika na kutoa machozi. 11 Walisikia
kwamba ni mzima na ameonekana naye, lakini hawakumwamini. 12 (Zingatia:
Nakala za kale hazina Marko 16: 9-20) Baada ya hayo, akajitokeza katika namna to-
fauti kwa watu wengine wawili, wakati walipokuwa wakitembea kutoka katika nchi.
13 Walienda na kuwaambia wanafunzi wengine waliobaki, lakini hawakuwaamini.
14 (Zingatia: Nakala za kale hazina Marko 16: 9-20) Yesu baadaye akajitokeza
kwa wale kumi na mmoja walipokuwa wameegama katika meza, na akawakemea
kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo, kwa sababu hawakuwaamini wale
waliomwona baada ya kufufuka kutoka kwa wafu. 15 Akawaambia, “ Enendeni
ulimwenguni mwote, na kuhubiri injili kwa viumbe vyote. 16 Yeyote aaminiye na
kubatizwa ataokolewa, na yule asiyeamini atahukumiwa. 17 (Zingatia: Nakala za kale
hazina Marko 16: 9-20) Ishara hizi zitaambatana na wote waaminio. Kwa jina langu
watatoa pepo. Watasema kwa lugha mpya. 18 Watashika nyoka kwa mikono yao, na
hata wakinywa kitu chochote cha kufisha hakitawadhuru. Wataweka mikono kwa
wagonjwa, nao watakuwa wazima”. 19 Baada ya Bwana kusema nao, akachukuliwa
juu mbinguni na ameketi mkono wa kuume wa Mungu. 20 Wanafunzi wakaondoka
na kuhubiri kila mahali, wakati Bwana akifanya kazi nao na kulithibitisha neno kwa
miujiza na ishara zikifuatana nao.

# Luka

1 Wengi wamejitahidi kuweka katika mpangilio simulizi kuhusu masuala ambayo
yametimizwa kati yetu, 2 kama walivyotupatia sisi, ambao tangu mwanzo ni
mashahidi wa macho na watumishi wa ujumbe. 3 Hivyo nami pia, baada ya
kuchuguza kwa uangalifu chanzo cha mambo haya yote tokea mwanzo - nimeona ni
vema kwangu pia kukuandikia katika mpangilio wake - mheshimiwa sana Theofilo.
4 Ili kwamba uweze kujua ukweli wa mambo uliyofundishwa. 5 Katika siku za
Herode, mfalme wa Yudea, palikuwa na kuhani fulani aliyeitwa Zekaria, wa ukoo
wa Abiya. Mke wake alitoka kwa binti za Haruni, na jina lake aliitwa Elizabeti.
6 Wote walikuwa wenye haki mbele za Mungu; walitembea bila lawama katika amri
zote na maagizo ya Bwana. 7 Lakini hawakuwa na mtoto, kwasababu Elizabethi
alikuwa tasa, na kwa wakati huu wote wawili walikuwa wazee sana. 8 Sasa
ilitokea kwamba Zakaria alikuwa katika uwepo wa Mungu, akiendelea na wajibu
wa kikuhani katika utaratibu wa zamu yake. 9 Kulingana na desturi ya kuchagua
ni kuhani yupi atakayehudumu, alikuwa amechaguliwa kwa kura kuingia katika
hekalu la Bwana na hivyo angefukiza uvumba. 10 Kundi lote la watu lilikuwa
likiomba nje wakati wa kufukizwa kwa ufumba. 11 Sasa malaika wa Bwana alimtokea
na kasimama upande wa kulia wa madhabahu ya kufukizia. 12 Zakaria alitishika
alipomuona; hofu ikamwangukia. 13 Lakini malaika akamwambia, “Usiogope
Zakaria, kwasababu maombi yako yamesikika. Mke wako Elizabeth atakuzalia
mwana. Jina lake utamwita Yohana. 14 Utakuwa na furaha na uchangamfu, na
wengi watakufurahia kuzaliwa kwake. 15 Kwa kuwa atakuwa mkuu mbele ya
macho ya Bwana. Hatakunywa divai au kinywaji kikali, na atakuwa amejazwa
na Roho Mtakatifu tangu tumboni mwa mama yake. 16 Na watu wengi wa Israel
watageuzwa kwa Bwana Mungu wao. 17 Atakwenda mbele za uso wa Bwana katika
roho na nguvu ya Eliya. Atafanya hivi ili kurejesha mioyo ya baba kwa watoto,
ili kwamba wasiotii wataenenda katika hekima ya wenye haki. Atafanya hivi
kuweka tayari kwa Bwana watu ambao wameandaliwa kwa ajili yake.” 18 Zakaria
akamwambia malaika, “Nitawezaje kujua hili? Kwasababu mimi ni mzee na mke
wangu miaka yake imekuwa mingi sana.” 19 Malaika akajibu na kumwambia, “Mimi
ni Gabrieli, ambaye husimama mbele za Mungu. Nilitumwa kukwambia, kukuletea
habari hii njema. 20 Na tazama, hutaongea, utakuwa kimya, hutaweza kuongea
mpaka siku ile mambo haya yatakapotokea. Hii ni kwasababu ulishindwa kuamini
maneno yangu ambayo yatatimizwa kwa wakati mwafaka.” 21 Sasa watu walikuwa
wakimsubiri Zakaria. Walishangazwa kwamba alikuwa anatumia muda mwingi
hekaluni. 22 Lakini alipotoka nje, hakuweza kuongea nao. Wakatambua kwamba
alikuwa amepata maono alipokuwa hekaluni. Aliendelea kuonesha ishara na alibaki
kimya. 23 Ikatokea kwamba siku za huduma yake zilipokwisha aliondoka kurudi
nyumbani kwake. 24 Baada ya Zakaria kurudi nyumbani kutoka kwenye huduma
yake hekaluni, mke wake akawa mjamzito. Naye hakutoka nyumbani mwake kwa
muda wa miezi mitano. Akasema, 25 “Hili ndilo amabalo Bwana amefanya kwangu
aliponitazama kwa upendeleo ili kuiondoa aibu yangu mbele za watu.” 26 Sasa,
katika mwezi wa sita wa mimba ya Elizabeti, Mungu alimwambia malaika Gabrieli
kwenda kwenye mji wa Galilaya uitwao Nazareti, 27 kwa bikra aliyekuwa ameposwa
na mwanaume ambaye jina lake lilikuwa Yusufu. Yeye alikuwa wa ukoo wa Daudi,
na jina la bikra huyo lilikuwa Mariamu. 28 Akaja kwake na akasema, “Salaam, wewe
uliyepokea neema kuu! Bwana amependezwa nawe.” 29 Lakini maneno ya malaika

yalimchanganya na hakuelewa kwa nini malaika alisema salaam hii ya ajabu kwake.
30 Malaika akamwambia, “Usiogope, Mariamu, maana umepata neema kutoka kwa
Mungu. 31 Na tazama, utabeba mimba katika tumbo lako na utazaa mwana. Nawe
utamwita jina lake 'Yesu.' 32 Atakuwa mkuu na ataitwa Mwana wa Aliye Juu Sana.
Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi baba yake. 33 Atatawala juu ya ukoo
wa Yakobo milele na ufalme wake hautakuwa na mwisho. 34 Mariamu akamwambia
malaika, hili litatokea kwa namna gani, maana sijawahi kulala na mwanaume yeyote?
35 Malaika akajibu na akamwambia, “Roho Mtakatifu atakujia juu yako, na nguvu ya
Aliye Juu Sana itakuja juu yako. Kwa hiyo, mtakatifu atakayezaliwa ataitwa Mwana
wa Mungu. 36 Na tazama, ndugu yako Elizabeti anaujauzito wa mwana kwenye umri
wake wa uzee. Huu ni mwezi wa sita kwake, ambaye alikuwa anaitwa mgumba.
37 Maana hakuna lisilowezekana kwa Mungu.” 38 Mariamu akasema, “Tazama, mimi
ni mtumishi wa kike wa Bwana. Acha iwe hivyo kwangu sawa sawa na ujumbe
wako.” Kisha malaika akamwacha. 39 Ndipo katika siku hizo Mariamu aliondoka
na kwa haraka alikwenda katika nchi ya vilima, kwenye mji katika nchi ya Yudea.
40 Alikwenda nyumbani mwa Zekaria na akamsalimia Elizabeti. 41 Sasa, ilitokea
kwamba Elizabeti aliposikia salamu ya Mariamu, mtoto tumboni mwake akaruka,
na Elizabeti akajazwa na Roho Mtakatifu. 42 Akapaza sauti yake na kusema kwa
sauti kuu, “umebarikiwa wewe zaidi miongoni mwa wanawake, na mtoto aliyemo
tumboni mwako amebarikiwa. 43 Na imekuwaje kwangu kwamba, mama wa Bwana
wangu ilipasa aje kwangu? 44 Kwa kuwa tazama, iliposikika masikoni mwangu
sauti ya kusalimia kwako, mtoto tumboni mwangu akaruka kwa furaha. 45 Na
amebarikiwe mwanamke yule ambaye aliamini ya kwamba ungetokea ukamilifu wa
mambo yale aliyoambiwa kutoka kwa Bwana.” 46 Mariamu akasema, nafsi yangu
inamsifu Bwana, 47 na roho yangu imefurahi katika Mungu Mwokozi wangu. 48 Kwa
maana ameiangalia hali ya chini ya mtumishi wake wa kike. Tazama, tangu sasa
katika vizazi vyote wataniita mbarikiwa. 49 Kwa maana yeye aliyemweza amefanya
mambo makubwa kwangu, na jina lake ni takatifu. 50 Rehema yake inadumu toka
kizazi hata kizazi kwa wale wanao mheshimu yeye. 51 Ameonesha nguvu kwa
mkono wake; amewatawanya wale ambao walijivuna juu ya mawazo ya mioyo
yao. 52 Amewashusha chini wana wa wafalme toka katika viti vyao vya enzi na
kuwainua juu walio na hali ya chini. 53 Aliwashibisha wenye njaa kwa vitu vizuri,
bali matajiri amewafukuza mikono mitupu. 54 Ametoa msaada kwa Israeli mtumishi
wake, ili kukumbuka kuonesha rehema 55 (kama alivyosema kwa baba zetu) kwa
Abrahamu na uzao wake milele.” 56 Mariamu alikaa na Elizabeti yapata miezi
mitatu hivi ndipo akarudi nyumbani kwake. 57 Sasa wakati ulikuwa umewadia kwa
Elizabeti kujifungua mtoto wake na akajifungua mtoto wa kiume. 58 Jirani zake na
ndugu zake walisikia jinsi Bwana alivyoikuza rehema kwake, na wakafurahi pamoja
naye. 59 Sasa ilitokea siku ya nane kwamnba walikuja kumtahiri mtoto. Ingewapasa
kumwita jina lake, “Zekaria,” kwa kuzingatia jina la baba yake, 60 Lakini mama
yake akajibu na kusema, “Hapana; ataitwa Yohana.” 61 Wakamwambia, hakuna hata
mmoja katika ndugu zako anayeitwa kwa jina hili.” 62 Wakamfanyia ishara baba yake
kuashiria yeye alitaka jina aitwe nani. 63 Baba yake akahitaji kibao cha kuandikia,
na akaandika, “Jina lake ni Yohana.” Wote wakashangazwa na hili. 64 Ghafla mdomo
wake ukafunguliwa na ulimi wake ukawa huru. Akaongea na kumsifu Mungu.
65 Hofu ikawajia wote walioishi karibu nao. Mambo haya yakaenea katika nchi
yote ya vilima vya Yudea. 66 Na wote walioyasikia wakayatunza mioyoni mwao,
wakisema, “ Mtoto huyu kuwa wa namna gani?” Kwasababu mkono wa Bwana
ulikuwa pamoja naye. 67 Baba yake Zekaria alijazwa na Roho Mtakatifu na akatoa
unabii, akisema, 68 “Asifiwe Bwana, Mungu wa Israeli, kwa sababu amesaidia na

alishughulikia wokovu kwa watu wake. 69 Ametuinulia pembe ya wokovu katika
nyumba ya mtumishi wake Daudi, kutoka miongoi mwa mwa ukoo wa mtumishi
wake Daudi, 70 kama alivyosema kwa kinywa cha manabii wake waliokuweko katika
nyakati za kale. 71 Atatuoka kutoka kwa adui zetu na kutoka mikononi mwa wote
wanaotuchukia. 72 Atafanya hivi kuonesha rehema kwa baba zetu, na kukumbuka
agano lake takatifu, 73 kiapo alichokisema kwa Abrahamu baba yetu. 74 Aliapa
kuthibitha kwamba ingewezekana kumtumikia Yeye bila hofu, baada ya kuokolewa
kutoka katika mikononi ya adui zetu. 75 katika utakatifu na haki mbele zake siku
zetu zote. 76 Ndiyo, na wewe mtoto, utaitwa nabii wa Aliye Juu Sana, kwa kuwa
utaenenda mbele za uso wa Bwana ili kumwandalia njia, kuwaandaa watu kwa
ajili ya ujio wake, 77 kuwafahamisha watu wake kwamba, wataokolewa kwa njia ya
kusamehewa dhambi zao. 78 Hili litatokea kwa sababu ya huruma ya Mungu wetu,
sababu ambayo jua tokea juu litatujia, 79 kuangaza kwao wakaao gizani na katika
uvuli wa mauti. Atafanya hivi kuiongoza miguu yetu kwenye njia ya amani.” 80 Sasa,
yule mtoto akakua na kuwa mwenye nguvu rohoni na alikaa nyikani mpaka siku ya
kujitokeza kwake kwa Israeli.

# 2

1 Sasa katika siku hizo, ikatokea kwamba Kaisari Agusto alitoa agizo akielekeza
kwamba ichukuliwe sensa ya watu wote wanaoishi duniani. 2 Hii ilikuwa ni sensa
ya kwanza iliyofanyika wakati Krenio akiwa gavana wa Siria. 3 Hivyo kila mmoja
akaenda mjini kwake kuandikishwa sensa. 4 Naye Yusufu aliondoka pia katika mji
wa Nazareti huko Galilaya na akasafiri Yudea katika mji wa Bethlehemu, ujulikanao
kama mji wa Daudi, kwa sababu alitokea katika ukoo ya Daudi. 5 Alikwenda
huko kujiandikisha pamoja na Mariamu, ambaye alikuwa amemposa na alikuwa
akitazamia mtoto. 6 Sasa ilitokea kwamba, wakiwa kule wakati wake wa kujifungua
mtoto ukawadia. 7 Akajifungua mtoto wa kiume, mzaliwa wake wa kwanza,
akamzungushia nguo mwilini kumkinga na baridi mtoto. Ndipo akamweka kwenye
kihori cha kulishia wanyama, kwa sababu haikuwepo nafasi kwenye nyumba za
wageni. 8 Katika eneo hilo, walikuwapo wachungaji walioishi mashambani wakilinda
makundi ya Kondoo wao usiku. 9 Ghafla, malaika wa Bwana akawatokea, na
utukufu wa Bwana ukang'aa kuwazunguka, na wakawa na hofu sana. 10 Ndipo
malaika akwaambia, “Msiogope, kwasababu nawaletea habari njema ambayo italeta
furaha kuu kwa watu wote. 11 Leo Mwokozi kazaliwa kwaajili yenu mjini mwa
Daudi! Yeye ndiye Kristo Bwana! 12 Hii ndiyo ishara ambayo mtapewa, mtamkuta
mtoto amefungwa nguo na amelala kwenye hori la kulishia wanyama.” 13 Ghafla
kukawa na jeshi kubwa la mbinguni likaungana na malaika huyo wakamsifu
Mungu, wakisema, 14 “Utukufu kwa Mungu aliye juu sana, na amani iwe duniani
kwa wote ambao anapendezwa nao.” 15 Ikawa kwamba malaika walipokwisha
kuondoka kwenda mbinguni, wachungaji wakasemezena wao kwa wao, “ Twendeni
sasa kule Bethlehemu, na tukaone hiki kitu ambacho kimetokea, ambacho Bwana
ametufahamisha.” 16 Wakaharakisha kule, na wakamkuta Mariamu na Yusufu, na
wakamuona mtoto amelala kwenye hori la kulishia wanyama. 17 Na walipoona
hivi, wakawajulisha watu kile walichokuwa wameambiwa kumhusu mtoto. 18 Wote
waliosikia habari hii wakashangazwa na kile kilichosemwa na wachungaji. 19 Lakini
Mariamu akaendelea kufikiri kuhusu yote aliyokwisha kuyasikia, akiyatunza moyoni
mwake. 20 Wachungaji wakarudi wakimtukuza na kumsifu Mungu kwa ajili ya
kila kitu walichokwisha sikia na kuona, kama tu ilivyokuwa imenenwa kwao.
21 Ilipofika siku ya nane na ilikuwa ni wakati wa kumtahiri mtoto, wakamwita jina
Yesu, jina alilokwishapewa na yule malaika kabla mimba haijatungwa tumboni.

22 zao zilizotakiwa za utakaso zilipopita, kulingana na sheria ya Musa, Yusufu
na Mariamu wakampeleka hekaluni kule Yerusalemu kumweka mbele za Bwana.
23 Kama ilivyoandikwa katika sheria ya Bwana, “Kila mwanaume anayefungua tumbo
ataitwa aliyetolewa wakfu kwa Bwana.” 24 Wao vilevile walikuja kutoa sadaka
kulingana na kile kinachosemwa katika sheria ya Bwana, “Jozi ya njiwa au makinda
mawili ya njiwa.” 25 Tazama, palikuwa na mtu katika Yerusalemu ambaye jina lake
alikuwa akiitwa Simeoni. mtu huyu alikuwa mwenye haki na mcha Mungu. Yeye
alikuwa akisubiri kwa ajili ya mfariji wa Israeli, na Roho Mtakatifu alikuwa juu
yake. 26 Ilikuwa imekwisha funuliwa kwake kupitia Roho Mtakatifu kwamba yeye
hangelikufa kabla ya kuwomwona Kristo wa Bwana. 27 Siku moja alikuja ndani
ya hekalu, akiongozwa na Roho Mtakatifu. Ambapo wazazi walimleta mtoto, Yesu,
kumfanyia yale yaliyopasa kawaida ya sheria, 28 ndipo Simeoni alimpokea mikononi
mwake, na akamsifu Mungu na kusema, 29 “Sasa ruhusu mtumishi wako aende
kwa amani Bwana, kulingana na Neno lako. 30 Kwa kuwa macho yangu yameuona
wakovu wako, 31 ambao umeonekana kwa macho ya watu wote. 32 Yeye ni nuru
kwa ajili ya ufunuo kwa Wamataifa na utukufu wa watu Israeli.” 33 Baba na Mama
wa mtoto walishangazwa kwa mambo ambayo yalizungumzwa juu yake. 34 Ndipo
Simeoni akawabariki na akasema kwa Mariamu mama yake, “Sikiliza kwa makini!
Mtoto huyu atakuwa sababu ya kupotea na kuokoka kwa watu wengi katika Israeli
na ni ishara ambayo watu wengi wataipinga. 35 Pia ni upanga utakaochoma nafsi
yako mwenyewe, ili kwamba mawazo ya mioyo ya wengi yadhihirike”. 36 Nabii
mwanamke aliyeitwa Ana pia alikuwako hekaluni. Yeye alikuwa binti wa Fanueli
kutoka kabila la Asheri. Alikuwa na miaka mingi sana. Naye aliishi na mume wake
kwa miaka saba baada ya kuoana, 37 na ndipo akawa mjane kwa miaka themanini
na minne. Naye hakuwahi kuondoka hekaluni na alikuwa akiendelea kumwabudu
Mungu pamoja na kufunga na kuomba, usiku na mchana. 38 Na kwa wakati huo,
alikuja pale walipo akaanza kumshukuru Mungu. Aliongea kumhusu mtoto kwa kila
mtu ambaye alikuwa akisubiri ukombozi wa Yerusalemu. 39 Walipomaliza kila kitu
walichotakiwa kufanya kuligana na na sheria ya Bwana, walirudi Galilaya, mjini
kwao, Nazareti. 40 Mtoto alikua, na akawa na nguvu, akiongezeka katika hekima,
na neema ya Mungu ilikuwa juu yake. 41 Wazazi wake kila mwaka walikwenda
Yerusalemu kwaajili ya sikukuu ya Pasaka. 42 Alipokuwa na umri wa miaka
kumi na miwili, walikwenda tena wakati mwafaka kidesturi kwa ajili ya sikukuu.
43 Baada ya kubaki siku zote kwa ajili ya sikukuu, walianza kurudi nyumbani.
Lakini mvulana Yesu alibaki nyuma mle Yerusalemu na wazazi wake hawakujua
hili. 44 Walidhani kwamba yumo kwenye kundi walilokuwa wakisafiri nalo, hivyo
walisafiri safari ya siku. Ndipo wakaanza kumtafuta miongoni wa ndugu na marafiki
zao. 45 Waliposhindwa kumpata, walirudi Yerusalemu na wakaanza kumtafuta
humo. 46 Ikatokea kwamba baada ya siku tatu, wakampata hekaluni, akiwa ameketi
katikati ya waalimu, akiwasikiliza na kuwauliza maswali. 47 Wote waliomsikia
walishangazwa na ufahamu wake na majibu yake. 48 Walipomwona, walistaajabu.
Mama yake akamwambia, “Mwanangu, kwa nini umetutendea hivi? Sikiliza, baba
yako na mimi tumekuwa tukikutafuta kwa wasiwasi mkubwa.” 49 Akawaambia,
“Kwa nini mmekuwa mkinitafuta? Hamkujua kwamba lazima niwe kwenye nyumba
ya Baba yangu? 50 Lakini hawakuelewa nini alichomaanisha kwa maneno hayo.
51 Ndipo akaenda pamoja nao mpaka nyumbani Nazareti na alikuwa mtii kwao.
Mama yake alihifadhi mambo yote moyoni mwake. 52 Lakini Yesu aliendelea kukua
katika hekima na kimo, na akazidi kupendwa na Mungu na watu.

# 3

[1] Sasa, katika mwaka wa kumi na tano wa utawala wa Kaisari Tiberia, wakati Pontio
Pilato alikuwa gavana wa Uyahudi, Herode alikuwa mkuu wa mkoa wa Galilaya, na
Filipo ndugu yake alikuwa mkuu wa mkoa wa Iturea na Trakoniti, na Lisania alikuwa
mkuu wa mkoa wa Abilene, [2] na wakati wa ukuhani mkuu wa Anasi na Kayafa,
Neno la Mungu lilimjia Yohana mwana wa Zakaria, jangwani. [3] Alisafiri katika
mkoa wote kuzunguka Mto Yordani, akihubiri ubatizo wa toba kwa ajili ya msamaha
wa dhambi [4] Kama ilivyoandikwa katika kitabu cha maneno ya Isaya nabii, "sauti
ya mtu aliaye nyikani, "Itengenezeni tayari njia ya Bwana, yatengenezeni mapito
yake yaliyoonyoka. [5] Kila bonde litajazwa, kila mlima na kilima vitasawazishwa,
barabara zilizopinda zitanyoshwa, na njia zilizoparaza zitalainishwa. [6] Watu wote
watauona wokovu wa Mungu." [7] Hivyo, Yohana akawaambia makutano makubwa
ya watu waliomjia wapate kubatizwa na yeye, "Ninyi uzao wa nyoka wenye sumu,
nani aliwaonya kuikimbia gadhabu inayokuja? [8] Zaeni matunda yanayoedana na
toba, na msianze kusema ndani yenu, "Tunaye Ibarahimu ambaye ni baba yetu;
kwa sababu nawaambia ya kwamba, Mungu anaweza kumwinulia Ibrahimu watoto
hata kutokana na mawe haya. [9] Tayari shoka limeshawekwa kwenye mzizi wa miti.
Hivyo, kila mti usiozaa matunda mema, hukatwa na kutupwa motoni. [10] Kisha watu
katika makutano walimuuliza wakisema, "Sasa tunatakiwa tufanyeje?" [11] Alijibu na
kuwaambia, "kama mtu ana kanzu mbili anatakiwa atoe kanzu moja kwa mwingine
ambaye hana kabisa, na ambaye ana chakula na afanye vivyo hivyo." [12] Kisha baadhi
ya watoza ushuru walikuja pia kubatizwa, na wakamwambia, "Mwalimu, tunatakiwa
kufanya nini? [13] Akawaambia, "Msikusanye fedha zaidi kuliko mnachotakiwa
kukusanya." [14] Baadhi ya maaskari pia wakamuuliza wakisema, "Na sisi je?
Tunatakiwa tufanye nini?" Akawambia, "Msichukue fedha kwa mtu yeyote kwa
nguvu, na msimtuhumu mtu yeyote kwa uongo. Ridhikeni na mishahara yenu."
[15] Sasa, kwa kuwa watu walikuwa na shauku ya kumngojea Kristo atakaye kuja, kila
mmoja alikuwa anawaza moyoni mwake kuhusu Yohana kama yeye ndiye Kristo.
[16] Yohana akajibu kwa kuwaambia wote, "Mimi nawabatiza ninyi kwa maji, lakini
kuna mmoja ajaye ambaye ana nguvu kuliko mimi, na sisitahili hata kufungua kamba
za viatu vyake. Atawabatiza ninyi kwa Roho Mtakatifu na kwa moto. [17] Pepeto
lake liko mkononi mwake ili kusafisha vizuri uwanda wake wa kupepetea ngano na
kuikusanya ngano ghalani mwake. Lakini, atayateketeza makapi kwa moto ambao
hauwezi kuzimika. [18] Kwa maonyo mengine mengi pia, alihubiri habari njema kwa
watu. [19] Yohana alimkemea pia Herode mkuu wa mkoa kwa kumuoa Herodia, mke
wa ndugu yake na kwa maovu mengine mengi ambayo Herode alikuwa ameyatenda.
[20] Lakini baadaye Herode alifanya uovu mwingine mbaya sana. Alimfunga Yohana
gerezani. [21] Kisha ilitokea kwamba, wakati watu wote walipokuwa wakibatizwa na
Yohana, naye Yesu alibatizwa pia. Wakati alipokuwa akiomba, mbingu zikafunguka.
[22] Roho Mtakatifu akashuka juu yake kwa mfano wa kiwiliwili kama njiwa, wakati
huo huo sauti ikaja kutoka mbinguni ikisema, "Wewe ni Mwanangu mpendwa.
Ninapendezwa sana na wewe." [23] Sasa Yesu mwenyewe, alipoanza kufundisha,
alikuwa na umri upatao miaka thelathini. Alikuwa ni mwana (kama ilivyotadhaniwa)
wa Yusufu, mwana wa Eli, [24] mwana wa Mathati, mwana wa Lawi, mwana wa Melki,
mwana wa Yana, mwana wa Yusufu, [25] mwana wa Matathia, mwana wa Amosi,
mwana wa Nahumu, mwana wa Esli, mwana wa Nagai, [26] mwana wa Maati, mwana
wa Matathia, mwana wa Semeini, mwana wa Yusufu, mwana wa Yuda, [27] mwana wa
Yoanani, mwana wa Resa, mwana wa Zerubabeli, mwana wa Shealtieli, mwana wa
Neri, [28] mwana wa Melki, mwana wa Adi, mwana wa Kosamu, mwana wa Elmadamu,
mwana wa Eri, [29] mwana wa Yoshua, mwana wa Eliezeri,, mwana wa Yorimu, mwana

wa Matathi, mwana wa Lawi, 30 mwana wa Simeoni, mwana wa Yuda, mwana wa
Yusufu, mwana wa Yonamu, mwana wa Eliyakimu, 31 mwana wa Melea, mwana wa
Mena, mwana wa Matatha, mwana wa Nathani, mwana wa Daudi, 32 mwana wa
Yese, mwana wa Obedi, mwana wa Boazi, mwana wa Salmoni, mwana wa Nashoni,
33 mwana wa Abinadabu, mwana wa Aramu, mwana wa Hesroni,, mwana wa Peresi,
mwana wa Yuda, 34 mwana wa Yakobo, mwana wa Isaka, mwana wa Ibrahimu,
mwana wa Tera, mwana wa Nahori, 35 mwana wa Seruig, mwana wa Ragau, mwana
wa Pelegi, mwana wa Eberi, mwana wa Sala, 36 mwana wa Kenani, mwana wa
Arfaksadi, mwana wa Shemu, mwana wa Nuhu, mwana wa Lameki, 37 mwana wa
Methusela, mwana wa Henoko, mwana wa Yaredi, mwana Mahalalei, mwana wa
Kenani, 38 mwana wa Enoshi, mwana wa Sethi, mwana wa Adamu, mwana wa
Mungu.

# 4

1 Kisha, Yesu akiwa amejaa Roho Mtakatifu, alirudi kutoka Mto Jordani, na
aliongozwa na Roho jangwani 2 kwa siku arobaini, na huko alijaribiwa na Ibilisi.
Wakati huo hakula chochote, na mwisho wa wakati huo alihisi njaa. 3 Ibilisi
akamwambia, “Kama wewe ni Mwana wa Mungu, liamru jiwe hili kuwa mkate.”
4 Yesu akamjibu, “Imeandikwa; 'mtu hataishi kwa mkate pekee.” 5 Kisha Ibilisi
alimwongoza juu kwenye kilele cha mlima, na akamwonyesha falme zote za dunia
kwa muda mfupi. 6 Ibilisi akamwambia, “Nitakupa mamlaka ya kutawala falme hizi
zote pamoja na fahari zake. Naweza kufanya hivyo kwa sababu vyote vimekabidhiwa
kwangu nivitawale, na ninaweza kumpa yeyote nitakaye kumpa. 7 Kwahiyo, kama
utaniinamia na kuniabudu, vitu hivi vyote vitakuwa vyako.” 8 Lakini Yesu alijibu
na kumwambia, “Imeandikwa, “lazima umwabudu Bwana Mungu wako, na lazima
umtumikie Yeye peke yake.” 9 Baadaye Ibilisi alimwongoza Yesu hadi Yerusalemu
na kumweka sehemu ya juu kabisa ya jengo la hekalu na kumwambia, “Kama
wewe ni Mwana wa Mungu, jitupe chini kutoka hapa. 10 Kwa sababu imeandikwa,
“Atawaagiza malaika zake wakutunze na kukulinda, 11 na watakuinua juu mikononi
mwao ili kwamba usiumize miguu yako juu ya jiwe.” 12 Yesu akijibu alimwambia,
“Imenenwa, “usimjaribu Bwana Mungu wako.” 13 Ibilisi alipomaliza kumjaribu Yesu,
aliенda zake na kumwacha hadi wakati mwingine. 14 Kisha Yesu alirudi Galilaya
kwa nguvu za Roho, na habari kumhusu yeye zikaenea na kusambaa katika mikoa
jirani yote. 15 Alifundisha katika masinagogi yao, na kila mmoja alimsifu. 16 Siku
moja alikwenda Nazareti, mji ambao alilelewa na kukulia. Kama ilivyokuwa desturi
yake aliingia kwenye sinagogi siku ya sabato, na alisimama kusoma maandiko.
17 Alikabidhiwa gombo la nabii Isaya, hivyo, alilifungua gombo na akatafuta sehemu
iliyoandikwa, 18 “Roho wa Bwana yuu juu yangu, kwa sababu alinitia mafuta kuhubiri
habari njema kwa maskini. Amenituma kutangaza uhuru kwa wafungwa, na
kuwafanya wasioona waweze kuona tena. Kuwaweka huru wale wanaogandamizwa,
19 kuutangaza mwaka ambao Bwana ataonesha wema wake.” 20 Kisha akalifunga
gombo, akamrudishia kiongozi wa sinagogi, na akaketi chini. Macho ya watu wote
waliokuwa katika sinagogi yalimwangalia yeye. 21 Alianza kuzungumza nao akisema,
“Leo andiko hili limetimizwa masikioni mwenu.” 22 Kila mmoja pale alishuhudia
kile alichokisema Yesu, na wengi miongoni mwao walishangazwa na maneno ya
hekima yaliyokuwa yakitoka katika kinywa chake. Walikuwa wakisema, “huyu ni
kijana tu wa Yusufu, siyo hivyo?” 23 Yesu akawaambia, “hakika mtasema methali hii
kwangu, “Tabibu, jiponye mwenyewe. Chochote tulichosikia ukifanya Kapernaumu,
kifanye hapa pia kijijini kwako.” 24 Pia alisema, “hakika nawaambia ninyi, hakuna
nabii anayekubalika katika nchi yake.” 25 Lakini nawaambia ninyi kweli kwamba
kulikuwa na wajane wengi Israel katika kipindi cha Eliya, wakati mbingu ilipofungwa

kusiwe na nvua kwa miaka mitatu na nusu, wakati kulipokuwa na njaa kubwa
katika nchi yote. 26 Lakini Eliya hakutumwa kwa yeyote mmoja wao, lakini kwa
mjane mmoja tu aliyeishi Sarepta karibu na mji wa Sidoni. 27 Pia, kulikuwa na
wakoma wengi Israel katika kipindi cha Elisha nabii, lakini hakuna hatammoja wao
aliyeponywa isipokuwa Naamani mtu wa Siria. 28 Watu wote ndani ya sinagogi
walijawa na gadhabu walipoyasikia haya yote. 29 Walisimama na kumsukumizia nje
ya mji, na kumwongoza mpaka kwenye ukingo wa mlima wa mji ambapo mji wao
ulijengwa juu yake, ili waweze kumtupa chini. 30 Lakini alipita salama katikati yao na
akaenda zake. 31 Kisha alitelemkia Kapernaumu, katika mji wa Galilaya. Sabato moja
alikuwa akifundisha watu ndani ya sinagogi. 32 Walishangazwa na mafundisho yake,
kwasababu alifundisha kwa mamlaka. 33 Sasa siku hiyo ndani ya sinagogi, kulikuwa
na mtu aliyekuwa na roho ya pepo mchafu, na alilia kwa sauti ya juu, 34 "Tuna nini
nawe, Yesu wa Nazareti? Umekuja kutuangamiza? Ninajua wewe ni nani! Wewe
ni mtakatifu wa Mungu!" 35 Yesu alimkemea pepo akisema, "Nyamaza kimya, na
umtoke mtu huyu!" Pepo yule alipomtupa mtu yule chini katikati yao, alimtoka
yule mtu bila ya kumsababishia maumivu yoyote. 36 Watu wote walishangaa, na
waliendelea kuzungumzia jambo hilo kila mmoja na mwenzake. Wakasema, "Ni
maneno ya aina gani haya?" Anawaamuru roho wachafu kwa mamlaka na nguvu
na watondoka." 37 Hivyo, habari juu ya Yesu zilienea kila sehemu katika maeneo
yanayozunguka mkoa huo. 38 Kisha Yesu aliondoka katika mji huo na akaingia
katika nyumba ya Simoni. Sasa, mama mkwe wake na Simoni alikuwa anaumwa
homa kali, na wakamsihi kwa niaba yake. 39 Hivyo, Yesu alimsogelea, akaikemea ile
homa na ikamwachia. Ghafla alisimama na akaanza kuwatumikia. 40 Jua lilipokuwa
likizama, watu walimletea Yesu kila mmoja aliyekuwa mgonjwa wa maradhi ya
aina mbalimbali. Aliweka mikono yake juu ya kila mgonjwa na akawaponya wote.
41 Mapepo pia yaliwatoka wengi wao yakilia kwa sauti na kusema, "Wewe ni mwana
wa Mungu!" Yesu aliwakemea mapepo na hakuwaruhusu waongee, kwa sababu
walijua kwamba yeye alikuwa ni Kristo. 42 Wakati kulipopambazuka, alienda eneo
lisilokuwa na watu. Makutano ya watu walikuwa wakimtafuta na wakaja katika
eneo alilokuwapo. Walijaribu kumzuia asiende mbali na wao. 43 Lakini akawaambia,
"Lazima pia nihubiri habari njema za ufalme wa Mungu katika miji mingine mingi,
kwa kuwa hii ndiyo sababu nilitumwa hapa." 44 Kisha aliendelea kuhubiri ndani ya
masinagogi katika uyahudi wote.

# 5

1 Basi ilitokea wakati watu walipomkusanyikia na kumzunguka Yesu na kusikiliza
neno la Mungu, ambapo alikuwa amesimama kando ya ziwa Genesareti. 2 Aliona
mashua mbili zimetia nanga pembeni mwa ziwa. Wavuvi walikuwa wametoka na
walikuwa wakiosha nyavu zao. 3 Yesu akaingia katika mojawapo ya zile mashua,
ambayo ilikuwa ya Simoni na kumwomba aipeleke majini mbali kidogo na nchi
kavu. Kisha akakaa na kufundisha kutokea kwenye mashua. 4 kuongea, akamwambia
Simoni, "Ipeleke mashua yako mpaka kwenye kilindi cha maji nakushusha nyavu
zako ili kuvua samaki." 5 Simon akajibu na kusema, Bwana, tumefanya kazi
usiku wote, na hatukukamata chochote, lakini kwa neno lako, nitazishusha nyavu.
6 Walipofanya hivyo walikusanya kiasi kikubwa cha samaki na nyavu zao zikaanza
kukatika. 7 Hivyo wakawaashiria washirika wao kwenye mashua nyingine ili waja
na kuwasaidia. Walikuja wakazijaza mashua zote, kiasi kwamba zikaanza kuzama.
8 Lakini Simoni Petro, alipoona hivyo, alianguka magotini pa Yesu akisema,"Ondoka
kwangu, kwa sababu mimi ni mtu mwenye dhambi Bwana." 9 Kwa sababu
alishangazwa, na wote waliokuwa pamoja naye, kwa uvuvi wa samaki waliokuwa

wameufanya. 10 Hili liliwajumuisha Yakobo na Yohana wana wa Zebedayo, ambao
walikuwa washirika wa Simoni. Na Yesu akamwambia Simoni, “Usiogope, kwa
sababu kuanzia sasa na kuendelea utavua watu.” 11 Walipokwishazileta mashua zao
nchi kavu, waliacha kila kitu na kumfuata yeye. 12 Ilitokea kwamba alipokuwa katika
mji mmojawapo, mtu aliyekuwa amejaa ukoma alikuwa huko. Wakati alipomuona
Yesu, alianguka akiinamisha uso kwake mpaka chini na kumuomba, akisema,
“Bwana, ikiwa unataka, waweza kunitakasa.” 13 Kisha Yesu alinyoosha mkono
wake na kumgusa, akisema, “Nataka. Takasika.” Na saa ileile ukoma ukamwacha.
14 “Alimwagiza asimwambie mtu yeyote, lakini alimwambia, “Nenda zako, na
ukajionyeshe kwa makuhani na utoe sadaka ya utakaso wako, sawasawa na kile Musa
alichokiamuru, kwa ushuhuda kwao.” 15 Lakini habari kumuhusu yeye zikaenea
mbali zaidi, na umati mkubwa wa watu ukaja pamoja kumsikiliza akifundisha na
kuponywa magonjwa yao. 16 Lakini mara kwa mara alijitenga faraghani na kuomba.
17 Ilitokea siku moja kati ya hizo siku alikuwa akifundisha, na walikuwapo Mafarisayo
na waalimu wa sheria wamekaa hapo ambao walikuja wakitokea vijiji vingi tofauti
katika mkoa wa Galilaya na Yudea, na pia kutokea katika mji wa Yerusalemu. Nguvu
ya Bwana ilikuwa pamoja naye kuponya. 18 watu kadhaa walikuja, wamembeba
kwenye mkeka mtu aliyepooza, na wakatafuta njia ya kumwingiza ndani ili kumlaza
chini mbele ya Yesu. 19 Hawakupata njia ya kumwingiza ndani kwa sababu ya umati,
hivyo walipanda juu ya paa la nyumba na kumshusha yule mtu chini kupitia kwenye
vigae, juu mkeka wake katikati ya watu, mbele kabisa ya Yesu. 20 Akiangalia imani
yao, Yesu alisema, “Rafiki, dhambi zako umesamehewa.” 21 Waandishi na Mafarisayo
waliaanza kuhoji hilo, wakisema, “Huyu ni nani anayeongea makufuru? Ni nani
anaweza kusamehe dhambi ila Mungu pekee yake?” 22 Lakini Yesu, akitambua nini
walichokuwa wakifikiri, aliwajibu na kuwaambia, “Kwa nini mnaulizana hili mioyoni
mwenu? 23 Kipi ni rahisi kusema, 'Dhambi zako zimesamehewa' au kusema 'Simama
utembee?' 24 Lakini mjue ya kwamba Mwana wa Adamu anayo mamlaka duniani
ya kusamehe dhambi, Nakwambia wewe, 'Amka, chukua mkeka wako na uende
nyumbani kwako.'” 25 Wakati huo huo akaamka mbele yao na akachukua mkeka
wake aliokuwa ameulalia. Kisha akariudi nyumbani kwake akimtukuza Mungu.
26 Kila mmoja alishangazwa na wakamtukuza Mungu. Walijawa na hofu, wakisema,
“Tumeona mambo yasiyo ya kawaida leo.” 27 Baada ya mambo haya kutokea, Yesu
alitoka huko na akamwona mtoza ushuru aliyeitwa Lawi amekaa eneo la kukusanyia
kodi. Akamwambia, “Nifuate.” 28 Hivyo Lawi akanyanyuka na kumfuata, akiacha kila
kitu nyuma. 29 Kisha Lawi akaandaa nyumbani kwake karamu kubwa kwa ajili ya
Yesu. Walikuwapo watozaushuru wengi kule na watu wengi walioketi mezani wakila
pamoja nao. 30 Lakini Mafarisayo na waandishi wao walikuwa wakiwanung'unikia
wanafunzi, wakisema, “Kwa nini mnakula na kunywa na watoza ushuru pamoja
na watu wengine wenye dhambi?” 31 Yesu akawajibu, “Watu walio katika afya
njema hawahitaji tabibu, ni wale tu wanaoumwa ndiyo watakao mhitaji mmoja.
32 Sikuja kuwaita watu wenye haki haki wapate kutubu, bali kuwaita wenye dhambi
wapate kutubu.” 33 Wakamwambia, “Wanafunzi wa Yohana mara nyingi hufunga na
kuomba, na wanafunzi wa Mafarisayo nao hufanya vivyo hivyo. Lakini wanafunzi
wako hula na kunywa.” 34 Yesu akawaambia, “Inawezekana mtu yeyote akawafanya
waliohudhuria harusi ya Bwana Arusi kufunga wakati Bwana Arusi bado yu pamoja
nao? 35 Lakini siku zitakuja wakati Bwana Arusi atakapoondolewa kwao, ndipo
katika siku hizo watafunga.” 36 Kisha Yesu aliongea pia kwao kwa mfano. “Hakuna
anayechana kipande cha nguo kutoka kwenye vazi jipya na kukitumia kurekebisha
vazi la zamani. Kama akifanya hivyo, ataichana nguo mpya, na kipande cha nguo
kutoka vazi jipya kisengefaa kutumika na nguo ya vazi la zamani. 37 pia, hakuna

mtu ambaye huweka divai mpya kwenye viriba vikuukuu. Kama akifanya hivyo,
divai mpya ingepasua kile chombo, na divai ingemwagika, na viriba vingeharibika.
38 Lakini divai mpya lazima iwekwe kwenye viriba vipya. 39 Na hakuna mtu baada ya
kunywa divai ya zamani, hutataka mpya, kwa sababu husema, 'Ya zamani ni bora."'

# 6

1 Sasa ilitokea kwenye Sabato kwamba Yesu alikuwa akipita katika ya shamba
la nafaka na wanafunzi wake walikuwa wakichuma masuke, wakayasuguasugua
kati ya mikono yao wakala nafaka. 2 Lakini baadhi ya Mafarisayo wakasema,
"Kwa nini mnafanya kitu ambacho si halali kisheria kukifanya siku ya sabato"?
3 Yesu, akawajibu, akisema, "Hamkuwahi kusoma kile Daudi alifanya alipokuwa
na njaa, yeye na wanaume waliokuwa pamoja naye? 4 Alikwenda katika nyumba
ya Mungu, na akachukuwa mikate mitakatifu na kuila baadhi, na kuitoa baadhi
kwa watu aliokuwa nao kuila, hatakama ilikuwa halali kwa makuhani kuila."
5 Kisha akawaambia, "Mwana wa Adamu ni Bwana wa Sabato." 6 Ilitokea katika
Sabato nyingine kwamba alikwenda ndani ya sinagogi na kuwafundisha watu huko.
Palikuwa na mtu ambaye mkono wake wa kulia ulikuwa umepooza. 7 Waandishi
na Mafarisayo walikuwa wanamwangalia kwa makini kuona kama angemponya
mtu siku ya Sabato, ili waweze kupata sababu ya kumshtaki kwa kufanya kosa.
8 Lakini alijua nini walikuwa wanafikiri na akasema kwa mtu aliyekuwa amepooza
mkono, "Amka, simama hapa katikati ya kila mmoja." Hivyo huyo mtu akanyanyuka
na kusimama pale. 9 Yesu akasema kwao, "Nawauliza ninyi, ni halali siku ya
Sabato kufanya mema au kufanya madhara, kuokoa maisha au kuyaharibu?"
Kisha aliwaangalia wote na kumwambia yule mtu, 10 "Nyoosha mkono wako."
Akafanya hivyo, na mkono wake ulikuwa umeponywa. 11 Lakini walijawa na
hasira, wakaongeleshana wao kwa wao kuhusu nini wanapaswa wafanye kwa Yesu.
12 Ilitokea siku hizo kwamba alikwenda mlimani kuomba. Aliendelea usiku mzima
kumuomba Mungu. 13 Ilipokuwa asubuhi, aliwaita wanafunzi wake kwake, na
akawachagua kumi na wawili kati yao, ambao pia aliwaita "mitume." 14 Majina
ya wale mitume yalikuwa Simoni (ambaye pia alimwita Petro) na Andrea ndugu
yake, Yakobo, Yohana, Filipo, Bartolomayo, 15 Mathayo, Tomaso na Yakobo mwana
wa Alfayo, Simoni, ambaye aliitwa Zelote, 16 Yuda mwana Yakobo na Yuda Iskariote,
ambaye alikuwa msaliti msaliti. 17 Kisha Yesu alitelemka pamoja nao toka mlimani
na kusimama mahali tambarare. Idadi kubwa ya wanafunzi wake walikuwa huko,
pamoja na idadi kubwa ya watu kutoka Uyahudi na Yerusalemu, na kutoka pwani
ya Tiro na Sidoni. 18 Walikuja kumsikiliza na kuponywa magonjwa yao. Watu
waliokuwa wakisumbuliwa na pepo wachafu waliponywa pia. 19 Kila mmoja
kwenye hilo kusanyiko alijaribu kumgusa kwa sababu nguvu za uponyaji zilikuwa
zikitokea ndani yake, na aliwaponya wote. 20 Kisha akawaangalia wanafunzi wake,
na kusema, "Mmebarikiwa ninyi mlio maskini, kwa maana ufalme wa Mungu
ni wenu. 21 Mmebarikiwa ninyi mlio na njaa sasa, kwa maana mtashibishwa.
Mmebarikiwa ninyi mliao sasa, kwa maana mtacheka. 22 Mmebarikiwa ninyi ambao
watu watakapowachukia na kuwatenga na kuwashutumu ninyi kwamba ni waovu,
kwa ajili ya Mwana Adamu. 23 Furahini katika siku hiyo na kurukaruka kwa furaha,
kwa sababu hakika mtakuwa na thawabu kubwa mbinguni, kwa maana baba zao
waliwatendea vivyohivyo manabii. 24 Lakini ole wenu mlio matajiri! Kwa maana
mmekwisha pata faraja yenu. 25 Ole wenu mlio shiba sasa! Kwa maana mtaona njaa
baadaye. Ole wenu mnaocheka sasa! Kwa maana mtaomboleza na kulia baadaye.
26 Ole wenu, mtakaposifiwa na watu wote! Kwa maana baba zao waliwatendea
manabii wa uongo vivyohivyo. 27 Lakini nasema kwenu ninyi mnaonisikiliza,

wapendeni adui zenu na kufanya mema kwa wanao wachukieni. [28] Wabarikini wale
wanao walaani ninyi na waombeeni wale wanaowaonea. [29] Kwake yeye akupigaye
shavu moja, mgeuzie na la pili. Kama mtu akikunyang'anya joho lako usimzuilie
na kanzu. [30] Mpe kila akuombaye. Kama mtu akikunyang'anya kitu ambacho
ni mali yako, usimuombe akurudishie. [31] Kama mpendavyo watu wawatendee,
nanyi watendeeni vivyo hivyo. [32] Kama mkiwapenda watu wawapendao ninyi tu,
hiyo ni thawabu gani kwenu? Kwamaana hata wenye dhambi huwapenda wale
wawapendao. [33] Kama mkiwatendea mema wale wanaowatendea ninyi mema,
hiyo ni thawabu gani kwenu? Kwa maana hata wenye dhambi hufanya vivyo
hivyo. [34] Kama mkikopesha vitu kwa watu ambao mnategemea watawarudishia,
hiyo ni thawabu gani kwenu? Hata wenye dhambi huwakopesha wenye dhambi,
na hutegemea kupokea kiasi hicho hicho tena. [35] Lakini wapendeni adui zenu na
watendeeni mema. Wakopesheni na msihofu kuhusu kurudishiwa, na thawabu
yenu itakuwa kubwa. Mtakuwa wana wa Aliye Juu, kwasababu yeye mwenyewe
ni mwema kwa watu wasio na shukurani na waovu. [36] Iweni na huruma, kama Baba
yenu alivyo na huruma. [37] Msihukumu, nanyi hamta hukumiwa. Msilaani, nanyi
hamtalaaniwa. Sameheni wengine, nanyi mtasamehewa. [38] Wapeni wengine, nanyi
mtapewa. Kiasi cha ukarimu - kilichoshindiliwa, kusukwasukwa na kumwagika
- kitamwagika magotini penu. Kwa sababu kwa kipimo chochote mnachotumia
kupimia, kipimo hicho hicho kitatumika kuwapimia ninyi.” [39] Kisha akawaambia
mfano pia. “Je mtu aliye kipofu aweza kumwongoza mtu mwingine kipofu?
Kama alifanya hivyo, basi wote wangalitumbukia shimoni, je wasingetumbukia?
[40] Mwanafunzi hawi mkubwa kuliko mwalimu wake, lakini kila mtu akiisha
kufundishwa kwa ukamilifu atakuwa kama mwalimu wake. [41] Na kwa nini basi
wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti lililo ndani
ya jicho lako huliangalii? [42] Utawezaje kumwambia ndugu yako, 'Ndugu, naomba
nikitoe kibanzi kilicho ndani ya jicho lako,' nawe huangalii boriti iliyo katika jicho
lako mwenyewe? Mnafiki wewe! Kwanza itoe boriti katika jicho lako mwenyewe,
ndipo utaona vizuri kutoa kibanzi katika jicho la ndugu yako. [43] Kwa sababu
hakuna mti mzuri uzaao matunda mabaya, wala hakuna mti mbaya uzaao matunda
mazuri. [44] Kwa sababu kila mti hutambulika kwa matunda yake. Kwa sababu
watu hawachumi tini kutoka kwenye miba, wala hawachumi zabibu kutoka kwenye
michongoma. [45] Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa yaliyo mema,
na mtu mwovu katika hazina mbovu ya moyo wake hutoa yaliyo maovu. Kwa sababu
kinywa chake husema yale yaujazayo moyo wake. [46] Kwanini mnaniita, 'Bwana,
Bwana', na bado hamyatendi yale nisemayo? [47] Kila mtu ajaye kwangu na kuyasikia
maneno yangu na kuyatendea kazi, nitawaonyesha jinsi alivyo. [48] Anafanana na mtu
ajengae nyumba yake, ambaye huchimba chini sana, na kujenga msingi wa nyumba
juu ya mwamba imara. Mafuriko yalipokuja, maporomoko ya maji yaliipiga nyumba,
lakini hayakuweza kuitikisa, kwa sababu ilikuwa imejengwa vizuri. [49] Lakini yeyote
asikiaye neno langu na hakulitii; mfano wake ni mtu aliyejenga nyumba juu ya
ardhi pasipokuwa na msingi, mto ulipoishukia kwa nguvu, nyumba ile ilitopata
maangamizi makubwa.

# 7

[1] Baada ya Yesu kumaliza kila kitu alichokuwa anasema kwa watu waliomsikiliza,
akaingia Kapernaumu. [2] Mtumwa fulani wa akida, aliyekuwa wa thamani sana
kwake, alikuwa mgonjwa sana na alikuwa karibu ya kufa. [3] Lakini akiwa
amesikia kuhusu Yesu, yule Akida alimtuma kiongozi wa kiyahudi, kumwomba aje
kumwokoa mtumwa wake ili asife. [4] Walipofika karibu na Yesu, walimsihi kwa

bidii na kusema, “anastahili kwamba unapaswa kufanya hivi kwa ajili yake, 5 kwa
sababu analipenda taifa letu, na ndiye aliyejenga sinagogi kwa ajili yetu”. 6 Yesu
akaendelea na safari yake pamoja nao. lakini kabla hajaenda mbali na nyumba,
afisa mmoja aliwatuma marafiki zake kuzungumza naye. “Bwana, usijichoshe
mwenyewe kwa sababu mimi sistahili wewe kuingia kwenye dari yangu. 7 Kwa
sababu hii sikufikiria hata mimi mwenyewe kuwa ninafaa kuja kwako, lakini sema
neno tu na mtumishi wangu atapona. 8 Kwani mimi pia ni mtu niliyewekwa
kwenye mamlaka na nina askari chini yangu. Husema kwa huyu “Nenda” na
huenda, na kwa mwingine, “Njoo” naye huja, na kwa mtumishi wangu 'Fanya hiki',
na yeye hufanya”. 9 Yesu aliposikia haya alishangaa, na kuwageukia makutano
waliokuwa wanamfuata na kusema.”Nawaambia, hata katika Israeli, sijawahi kuona
mtu mwenye imani kuu kama huyu. 10 Kisha wale waliokuwa wametumwa walirudi
nyumbani na kumkuta mtumishi akiwa mzima. 11 fulani baada ya haya, ilitokea
kuwa Yesu alikuwa anasafiri kwenda mji ulioitwa Naini. wanafunzi wake wakaenda
pamoja naye wakiambana na umati wa watu. 12 Alipofika karibu na Lango la
jiji tazama, mtu aliyekufa alikuwa amebebwa, na ni mtoto wa pekee kwa mama
yake. aliyekuwa mjane, na umati wa wawakilishi kutoka kwenye jiji walikuwa
pamoja naye. 13 Alipomwona, Bwana akamsogelea kwa huruma kubwa sana juu
yake na akamwambia, “Usilie”. 14 Kisha akasogea mbele akaligusa jeneza ambalo
walibebea mwili, na wale waliobeba wakasimama akasema “Kijana nasema amka”
15 Mfu akainuka na kukaa chini na akaanza kuongea. Kisha Yesu akamkabidhi
kwa mama yake. 16 Kisha hofu ikawajaa wote. wakaendelea kumtukuza Mungu
wakisema “Nabii mkuu ameinuliwa miongoni mwetu” na “Mungu amewaangalia
watu wake” 17 Hizi habari njema za Yesu zilienea Yudea yote na kwa mikoa yote
ya jirani. 18 Wanafunzi wa Yohana walimwamwambia mambo haya yote. 19 Ndipo
Yohana akawaita wawili wa wanafunzi wake na kuwatuma kwa Bwana kusema
“Wewe ndiye yule ajaye, au kuna mtu mwingine tumtazamie? 20 Walipofika karibu
na Yesu hawa wakasema, “Yohana mbatizaji ametutuma kwako kusema, 'Wewe ni
yule ajaye au kuna mtu mwingine tumtazamie?” 21 kwa wakati huo aliowaponya
watu wengi kutoka katika magonjwa na mateso, kutoka kwa roho wachafu, na kwa
watu wenye upofu aliwapa kuona. 22 Yesu akajibu na kusema kwao. “Baada ya
kuwa mmekwenda mlikotoka mtamjulisha Yohana mlichokiona na kukisikia. Wenye
upofu wanapokea kuona na viwete wanatembea, wenye ukoma wanatakasika, viziwi
wanasikia, wafu wanafufuliwa na kuwa hai tena, masikini wanaambiwa habari
njema. 23 Na mtu ambaye hataacha kuniamini mimi kwa sababu ya matendo yangu
amebarikiwa”. 24 Baada ya wale waliotumwa na Yohana kurudi walikotoka, Yesu
akaanza kusema kwa makutano juu ya Yohana, “Mlikwenda nje kuona nini, mwanzi
ukiwa unatikiswa na upepo? 25 lakini mlikwenda nje kuona nini, mtu aliyevaa
vizuri? tazama watu wale wanaovaa mavazi ya kifalme na kuishi maisha ya starehe
wako kwenye nafasi za wafalme. 26 lakini mnakwenda nje kuona nini, Nabii?
Ndiyo, ninasema kwenu na zaidi sana kuliko nabii. 27 Huyu ndiye aliyeandikiwa,
“Tazama, namtuma mjumbe wangu mbele ya macho yenu, atakeyeandaa njia kwa
ajili yangu, 28 Nasema kwenu, kati ya wale waliozaliwa na mwanamke, hakuna mkuu
kama Yohana, lakini mtu asiye muhimu sana atakayeishi na Mungu mahali alipo
yeye, atakuwa mkuu kuliko Yohana.” 29 Na watu wote waliposikia haya pamoja
na watoza ushuru, walitangaza kuwa Mungu ni mwenye Haki. Walikuwepo kati
yao wale waliobatizwa kwa ubatizo wa Yohana. 30 Lakini mafarisayo na wataalamu
wa sheria za kiyahudi, ambao hawakubatizwa na yeye walikataa hekima za Mungu
kwa ajili yao wenyewe. 31 Tena naweza kuwalinganisha na nini watu wa kizazi
hiki? Wakoje hasai? 32 Wanafanana na watoto wanaocheza kwenye eneo la soko,

wanaokaa na kuitana mmoja baada wa mwingine wakisema, 'Tumepuliza filimbi
kwa ajili yenu, na hamkucheza. tumeomboleza na hamkulia.' 33 Yohana mbatizaji
alikuja hakula mkate wala hakunywa divai, na mkasema "Ana pepo. 34 Mwana wa
Mtu amekuja amekula na kunywa na mkasema, "Angali ni mlafi na mlevi, rafiki
wa watoza ushuru na wenye dhambi! 35 Lakini hekima imetambulika kuwa ina
haki kwa watoto wake wote." 36 Mmoja wa mafarisayo alimwomba Yesu aende
kula pamoja naye. Baada ya Yesu kuingia kwenye nyumba ya farisayo, aliegemea
kwenye meza ili ale. 37 Tazama kulikuwa na mwanamke mmoja katika jiji hilo
aliyekuwa na dhambi. Akagundua kuwa alikuwa amekaa kwa Farisayo, akaleta
chupa ya manukato. 38 Alisimama nyuma yake karibu na miguu yake huku akilia.
Tena alianza kulowanisha miguu yake kwa machozi, na kuifuta kwa nywele za
kichwa chake, akiibusu miguu yake na kuipaka manukato. 39 Na yule farisayo
aliyekuwa amemwalika Yesu alipoona hivyo, akawaza mwenyewe akisema, "Kama
huyu mtu angekuwa nabii, angejua huyu ni nani na ni aina gani ya mwanamke
anayemgusa, ya kuwa ni mwenye dhambi. 40 Yesu akajibu na kumwambia, "Simoni
nina kitu cha kukuambia. "Akasema" "Kiseme tu mwalimu!" 41 Yesu akasema
"Kulikuwa na wadaiwa wawili kwa mkopeshaji mmoja. Mmoja alikuwa anadaiwa
dinari mia tano na wa pili alidaiwa dinari hamsini. 42 Na walipokuwa hawana pesa
ya kumlipa aliwasamehe wote. Sasa ni nani atampenda zaidi? 43 Simoni akamjibu
na kusema, "Nadhani aliyesamehewa zaidi."Yesu akamwambia, "Umehukumu kwa
usahihi." 44 Yesu akamgeukia mwanamke na kusema kwa Simoni, "Unamwona huyu
mwanamke. Nimeingia kwenye Nyumba yako. Hukunipa maji kwa ajili ya miguu
yangu, lakini huyu, kwa machozi yake, alilowanisha miguu yangu na kuifuta kwa
nywele zake. 45 Hukunibusu, lakini yeye, tangu alipoingia humu hakuacha kunibusu
miguu yangu. 46 Hukuipaka miguu yangu kwa mafuta, lakini ameipaka miguu yangu
kwa manukato. 47 Kwa jambo hili, nakwambia kwamba alikuwa na dhambi nyingi na
amesamehewa zaidi, na pia alipenda zaidi. Lakini aliyesamehewa kidogo, hupenda
kidogo tu." 48 Baadaye akamwambia mwanamke, "Dhambi zako zimesamehewa"
49 Wale waliokaa mezani pamoja naye wakaanza kusemezana wao kwa wao, "Huyu
ni nani mpaka anasamehe dhambi?" 50 Na Yesu akamwambia mwanamke, "Imani
yako imekuokoa. Enenda kwa amani"

# 8

1 Ilitokea muda mfupi baadaye kwamba Yesu alianza kusafiri katika miji na
jiji mbalimbali, akihubiri na kutangaza habari njema ya ufalme wa Mungu na
wale kumi wawili walikwenda pamoja naye, 2 vilevile wanawake fulani waliokuwa
wameponywa kutoka kwa roho wachafu na magonjwa mbalimbali. Walikuwa ni
Mariamu aliyeitwa Magdalena ambaye alikuwa ametolewa pepo saba. 3 Yoana mke
wa Kuza na meneja wa Herode, Susana, na wanawake wengine wengi, waliotoa mali
vyao kwa ajili yao wenyewe. 4 Nabaada ya umati wa watu kukusanyika pamoja,
wakiwemo na watu waliokuja kwake kutoka miji mbalimbali, akazungumza nao kwa
kutumia mifano. 5 "mpandaji alienda kupanda mbegu, alipokuwa apanda, baadhi
ya mbegu hizo ziliangukia kando ya njia zikakanyagwa chini ya miguu, na ndege
wa angani wakazila. 6 Mbegu zingine zilianguka juu ya udongo wa miamba na
zilipoota na kuwa miche zilipooza kwa sababu hakukuwa na unyevunyevu. 7 Mbegu
zingine ziliangukia kwenye miti ya miiba, nayo hiyo miti ya miiba ikakua pamoja
na zile mbegu na zikasongwa. 8 Lakini mbegu zingine ziliangukia kwenye udongo
unaofaa na zikazaa mazao mara mia zaidi. "Baada ya Yesu kusema mambo haya,
alipaza sauti,"Yeyote aliye na masikio ya kusikia na asikie." 9 Tena wanafunzi wake
wakamuuliza maana ya mfano huo, 10 Yesu akawaambia, "Mmepewa upendeleo wa

kujua siri ya ufalme wa Mungu, lakini watu wengine watafundishwa tu kwa mifano,
ili kwamba 'wakiona wasione na wakisikia wasielewe.' [11] Na hii ndiyo maana ya
mfano huu. Mbegu ni neno la Mungu. [12] Mbegu zile zilizoanguka kando kando ya njia
ndiyo wale watu wanaolisikia neno, na baadaye mwovu shetani hulichukua mbali
kutoka moyoni, ili kwamba wasiamini na kuokolewa. [13] Kisha na zile zilizoangukia
kwenye mwamba ni watu wale wanaosikia neno na kulipokea kwa furaha lakini
hawana mizizi yeyote, wanaamini tu kwa muda mfupi, na wakati wa majaribu
huanguka. [14] Na mbegu zile zilizoangukia kwenye miiba ni watu wanaosikia neno,
lakini wanapoendelea kukua husongwa na huduma na utajiri na ubora wa maisha
haya na hawazai matunda. [15] Lakini zile mbegu zilizoangukia kwenye udongo mzuri
ni wale watu, ambao ni wanyeyekevu na mioyo mizuri, baada ya kulisikia neno
hulishikilia na likawa salama na kuazaa matunda ya uvumilivu. [16] Sasa, hakuna
hata mmoja, anayewasha taa na kuifunika kwa bakuli au kuiweka chini ya kitanda.
Badala ya kuiweka kwenye kinara cha taa ili kwamba kila mmoja anayeingia apate
kuiona. [17] Kwa kuwa hakuna kitakachojificha ambacho hakitajulikana, au chochote
kilicho sirini ambacho hakitajulikana kikiwa kwenye mwanga. [18] kwa hiyo kuwa
makini unapokuwa unasikiliza. Kwa sababu aliye nacho, kwake ataongezewa zaidi,
lakini asiye nacho hata kile kidogo alicho nacho kitachukuliwa.” [19] baadaye mama
yake Yesu na ndugu zake wakaja kwake hawakaribia kwa sababu ya umati wa
watu. [20] Na akataarifiwa, “Mama yako na ndugu zako wako pale nje wanahitaji
kukuona wewe. [21] Lakini, Yesu akajibu akasema “Mama yangu na ndugu zangu ni
wale wanaolisikia neno la Mungu na kulitii.” [22] Ilitokea siku moja kati ya siku zile
Yesu na wanafunzi wake alipanda kwenye mtumbwi, na akawaambia, “Na tuvuke
ng'ambo ya pili ya ziwa.” Wakaandaa mashua yao. [23] Lakini walipoanza kuondoka,
Yesu akalala usingizi, na dhoruba kali yenye upepo, na mashua yao ikaanza kujaa
maji na walikuwa kwenye katika kubwa sana. [24] baadaye wanafunzi wake wakaja
kwake na kumwamsha, wakisema, “Bwana mkubwa! Bwana mkubwa! tuko karibu
kufa!” Akaamka na akaukemea upepo na mawimbi ya maji vikatulia na kukawa
na utulivu. [25] Tena akawaambia, “Imani yenu iko wapi?” Wakaogopa, Walishangaa,
wakasemezana kia mmoja na mwenzake,”Huyu ni nani, kiasi kwamba anaamuru
hata upepo, na maji na humtii?” [26] Wakafika kwenye mji wa Gerasini iliyo upande
wa nyuma ya Galilaya. [27] Yesu aliposhuka na kukanya kwenye ardhi, mtu fulani
kutoka mjini, akakutana naye, na huyu mtu alikuwa na nguvu za giza. Kwa muda
mrefu alikuwa havai nguo, na alikuwa haishi kwenye Nyumba, lakini aliishi kwenye
makaburi. [28] Alipomwona Yesu akalia kwa sauti, na akaanguka chini mbele yake.
kwa sauti kubwa akisema, Nimefanya nini kwako, Yesu mwana wa Mungu aliye
juu? Nakusihi, Usiniadhibu mimi” [29] Yesu akaamuru roho chafu imtoke mtu yule,
kwa kuwa mara nyingi amepamgaa. hata kama alikuwa amefungwa minyororo na
kubanwa na kuwekwa chini ya ulinzi, alivunja vifungo na kuendeshwa na mapepo
mpaka jangwani. [30] Yesu akamwuliza, “Jina lako nani?” akajibu akisema, “Legioni”
Kwa maana mapepo mengi yameingia kwake. [31] Wakaendelea kumsihi usituamuru
twende kwenye shimo. [32] Kundi la Nguruwe lilikuwa likichunga juu ya kilima,
wakamsihi awaruhusu wakaingie kwa hao nguruwe. Na akawaruhusu kufanya
hivyo. [33] kwa hiyo wale mapepo wakamtoka mtu yule na kuingia kwa wale nguruwe,
na lile kundi likakimbia kwenye mwinuko wa mlima mpaka ziwani na wakazama
humo. [34] wale watu waliokuwa wanachunga wale nguruwe walipoona kilichotokea,
wakakimbia na wakatoa taarifa pale mjini na nje katika miji iliyowazunguka. [35] Watu
waliposikia hayo walienda kuona kilichotokea, na wakaja kwa Yesu na wakamwona
mtu ambaye mapepo yalikuwa yamemtoka. alikuwa amevaa vizuri na mwenye
akili timamu, amekaa kwenye miguu ya Yesu, na waliogopa. [36] ndipo mmoja

wao aliyeona kilichotokea alianza kuwasimlia wengine jinsi huyu mtu aliyekuwa
anaongozwa na mapepo alivyoponywa. 37 Watu wote wa mkoa wa Wagerasi na
maeneo yaliyozunguka walimwomba Yesu aondoke kwao kwa sababu walikuwa na
hofu kuu. Na aliingia kwenye mtumbwi ili arudi. 38 Mtu yule aliyetokwa na pepo
alimsihi Yesu kwenda naye, lakini Yesu alimwambia aende na kusema, 39 "Rudi
kwenye nyumba yako na uhesabu yale yote ambayo Mungu amekutendea" Huyu
mtu aliondoka, akitangaza pote katika mji wote yale yote ambayo Yesu aliyofanya
kwa ajili yake. 40 Na Yesu akarudi, makutano wakamkaribisha, kwa sababu wote
walikuwa wanamngoja. 41 Tazama akaja mtu mmoja anaitwa Yairo ni mmoja kati
ya viongozi katika sinagogi. Yairo akaanguka miguuni pa Yesu na kumsihi aende
nyumbani kwake, 42 kwa sababu alikuwa na mtoto msichana mmoja tu, mwenye
umri wa miaka kumi na wibili, na alikuwa katika hali ya kufa. Na alipokuwa
akienda, makutano walikuwa wakisongama dhidi yake. 43 Mwanamke mwenye
kutokwa damu kwa miaka kumi na miwili alikuwa pale na alitumia pesa zote kwa
waganga, lakini hakuna aliyemponya hata mmoja, 44 alikuja nyuma ya yesu na
kugusa pindo la vazi lake, na ghafla kutokwa damu kukakoma. 45 Yesu akasema,
"Nani ambaye kanigusa?" Walipokataa wote, Petro akasema, Bwana Mkubwa, umati
wa watu wanakusukuma na wanakusonga." 46 Lakini Yesu akasema, "Mtu mmoja
alinigusa, maana nilijua nguvu zimetoka kwangu." 47 Mwanamke alipoona ya kuwa
hawezi kuficha alichokifanya, akaanza kutetemeka, akaanguka chini mbele za Yesu
alitangaza mbele ya watu wote sababu zilizofanya amguse na vile alivyoponywa
gafla. 48 Kisha akasema kwake, "Binti, imani yako imekufanya uwe mzima. Enenda
kwa Amani." 49 Alipokuwa akiendelea kusema, mtu mmoja akaja kutoka kwenye
nyumba ya kiongozi wa sinagogi, akisema, "Binti yako amefariki. Usimsumbue
mwalimu." 50 Lakini Yesu aliposikia hivyo, alimjibu, "Usiogope. Amini tu, na
ataokolewa." 51 Kisha alipoingia kwenye hiyo nyumba, hakuruhusu mtu yeyote
kuingia pamoja naye, isipokuwa Petro, Yohana na Yakobo, baba yake binti, na mama
yake. 52 Sasa watu wote walikuwa wanaomboleza na kutoa sauti kwa ajili yake, lakini
akasema, "Msipige kelele, hajafa, lakini amelala tu." 53 Lakini wakamcheka kwa
dharau, wakijua kuwa amekufa. 54 Lakini Yeye, akimshika binti mkono, akaita kwa
sauti, akisema, "Mtoto, inuka" 55 roho yake ikamrudia, na akainuka wakati huohuo.
Akaamrisha kwamba, apewe kitu furani kwa ili ale. 56 Wazazi wake wakashangaa,
lakini aliwaamuru wasimwambie mtu kilichokuwa kimetokea.

# 9

1 Akawaita wale kumi na wawili pamoja, akawapa uwezo na mamlaka juu ya
mapepo yote na kuponya magonjwa. 2 Akawatuma waende kuhubiri ufalme wa
Mungu na kuponya wagonjwa. 3 Akawaambia, "Msichukue chochote kwa ajili
ya safari yenu wala fimbo, wala mkoba, wala mkate, wala pesa wala msichukue
kanzu mbili. 4 Nyumba yoyote mtakayo iingia, kaeni humo mpaka mtakapo
ondoka mahali hapo. 5 Na kwa wale wasio wapokea, mtakapo ondoka mji huo,
jikung'uteni vumbi katika miguu yenu kwa ushuhuda juu yao". 6 Wakaondoka na
kwenda kupitia vijijini, wakitangaza habari njema na kuponya watu kila mahali.
7 Sasa Herode, mtawala, alisikia yote yaliyo kuwa yakitokea alitaabika sana, kwa
sababuu ilisemekana na baadhi kwamba Yohana mbatizaji amefufuka kutoka wafu,
8 na baathi kwamba Elia amekwisha tokea, na kwa wengine kwamba mmoja wa
manabii wa zamani amefufuka katika wafu tena. 9 Herode alisema, "nilimchinja
Yohana, lakini huyu ni nani ninae sikia habari zake? Na Herode alitafuta njia
ya kumwona Yesu. 10 Wakati waliporudi wale waliotumwa, wakamwamwambia
kila kitu walicho fanya. Akawachukua pamoja naye, akaenda peke yake katika

mji uitwao Bethsadia. 11 Lakini makutano wakasikia kuhusu hili wakamfuata, na aliwakaribisha, na akaongea nao kuhusu ufalme wa Mungu, na aliwaponya wale waliohitaji uponyaji. 12 Siku ikaanza kuisha, na wale kumi na wawili wakaenda kwake na kusema, "Watawanye makutano kwamba waende katika vijiji vya karibu na mijini wakatafute mapumziko na chakula, kwa sababu tupo eneo la nyikani."
13 Lakini akawaambia, "Nyie wapeni kitu cha kula." Wakasema "Hatuna zaidi ya vipande vitano vya mikate na samaki wawili, isipokuwa tungeenda na kununua chakula kwa ajili ya kusanyiko hili la watu." 14 Kulikua na wanaume wapatao elfu tano pale. Akawambia wanafunzi wake. "Wakalisheni chini katika makundi ya watu wapatao hamsini kwa kila kundi. 15 Kwa hiyo wakafanya hivyo na watu wa wakaketi chini. 16 Akachukua mikate mitano na samaki wawili na akatazama mbinguni, akavibariki, na kuvimega katika vipande, akawapa wanafunzi wake ili waviweke mbele ya makutano. 17 Wote wakala na wakashiba, na vipande vya chakula vilivyo baki viliokotwa na kujaza vikapu kumi na viwili. 18 Nayo ikawa kwamba, alipokuwa akiomba peke yake, wanafunzi wake walikuwa pamoja naye, na akawauliza akisema, "watu husema mimi ni nani?" 19 Wakijibu, wakasema, "Yohana mbatizaji, lakini wengine husema Eliya, na wengine husema mmoja wa manabii wa nyakati za zamani amefufuka tena." 20 Akawambia, "Lakini ninyi mwasema mimi ni nani?" Akijibu Petro akasema, "Kristo kutoka kwa Mungu." 21 Lakini kwa kuwaonya, Yesu akawaelekeza kutomwambia yeyote juu ya hili, 22 akasema kwamba mwana wa Adamu lazma ateseke kwa mambo mengi na kukataliwa na wazee na Makuhani wakuu na waandishi, na atauawa, na siku ya tatu atafufuka.
23 Akawambia wote, "kama mtu yeyote akitaka kunifuata, lazima ajikane mwenyewe, achukue msalaba wake kila siku, na anifuate. 24 Yeyote ajaribuye kuyaokoa maisha yake atayapoteza, lakini yeyote apotezae maisha yake kwa faida yangu, atayaokoa.
25 Je kitamfaidia nini mwanadamu, kama akiupata ulimwengu wote, lakini akapoteza au akapata hasara ya nafsi yake? 26 Yeyote atakaye nionea aibu mimi na maneno yangu, kwake yeye mwana wa Adam atamuonea aibu atakapo kuwa katika utukufu wake, na utukufu wa Baba na malaika watakatifu. 27 Lakini ninawaambia ukweli, kuna baadhi yenu wasimamao hapa, hawata onja umauti mpaka wauone ufalme wa Mungu." 28 Ikatokea yapata siku nane baada ya Yesu kusema maneno haya kwamba akawachukua pamoja nae Petro, Yohana na, Yakobo, wakapanda mlimani kuomba. 29 Na alipokuwa katika kuomba, muonekano wa uso wake ulibadilika, na mavazi yake yakawa meupe na ya kung'aa. 30 Na tazama, walikuwepo wanaume wawili wakiongea naye! Walikuwa Musa na Elia, 31 walionekana katika utukufu. Waliongea kuhusu kuondoka kwake, jambo ambalo alikaribia kulitimiza Yerusalem.
32 Sasa Petro na wale waliokua pamoja naye walikuwa katika usingizi mzito. Lakini walipokuamka, waliuona utukufu wake na wanaume wawili waliokuwa wamesimama pamoja nae. 33 Ikatokea kwamba, walipokuwa wakiondoka kwa Yesu, Petro akamwambia, "Bwana, ni vizuri kwetu kukaa hapa na inatupasa tutengeneze makazi ya watu watatu. Tutengeneze moja kwa ajili yako, moja kwa ajili ya Musa, na moja kwa ajili ya Eliya." Hakuelewa alichokuwa akiongelea. 34 Alipokuwa akisema hayo, likaja wingu na likawafunika; na waliogopa walipoona wamezunguwa na wamezungukwa na wingu. 35 Sauti ikatoka kwenye wingu ikasema, "Huyu ni Mwanangu mteule. Msikilizeni yeye." 36 Sauti iliponyamaza, Yesu alikuwa peke yake. walikaa kimya, na katika siku hizo hawakumwambia yeyote lolote miongoni mwa waliyoyaona. 37 Siku iliyofuata, baada ya kutoka mlimani, kusanyiko kubwa la watu lilikutana naye. 38 Tazama, mwanaume kutoka kwenye kusanyiko alilia kwa sauti, akisema, "Mwalimu ninakuomba umtazame mwanangu, kwa kuwa ni mwanangu wa pekee. 39 Unaona roho chafu humshika, na mara hupiga kelele,

na pia humfanya achanganyikiwe na kutokwa povu kinywani. Nayo humtoka
kwa shida, ikimsababshia maumivu makali. 40 Naliwasihi wanafunzi wako kuikea
itoke. lakini hawakuweza." 41 Yesu akajibu akasema, "Enyi kizazi kisichoamini
na kilichopotoka, mpaka lini nitkaa nanyi na kuchukuliana nanyi? Mlete mwanao
hapa." 42 Kijana aliokuwa anakuja, roho cha ikamuangusha chini na kumtikisa kwa
fujo. Lakini Yesu aliikemea ile roho chafu, alimponya mvulana, na kamkabidhi
kwa baba yake. 43 Wote walishangazwa na ukuu wa Mungu. Lakini walipokuwa
wakistaajabu wote kwa mambo yote aliyo yaliyotedeka, akasema kwa wanafunzi
wake, 44 "Maneno yawakae masikioni mwenu, kwa kuwa Mwana wa Adamu
atatolewa mikononi mwa wanadamu." 45 Lakni hawakuelewa maana ya maneno
hayo, na yalifichwa machoni pao, ili wasije wakalielewa. Waliogopa kumuuliza
kuhusu neno hilo. 46 Kisha mgogoro ulianza ulizuka miongoni mwao i juu ya nani
angekuwa mkuu. 47 Lakini Yesu alipotambua walichokuwa wakihojiana mioyoni
mwao, alimchukua mtoto mdogo, na kumuweka upande wake, 48 na akasema, " kama
mtu yeyote akimpokea mtoto mdogo kama huyu kwa jina langu, anipokea mimi
pia, na yeyote akinipokea mimi, ampokea pia aliyenituma, kwa kuwa aliye mdogo
kati yenu wote ndiye alie mkuu" 49 Yohana akajibu akasema, "Bwana, tulimuona
mtu akifukuza pepo kwa jina lako na tukamzuia, kwa sababu haambatani na sisi."
50 Lakini Yesu akamwambia, "Msimzuie, kwa kuwa asiye kinyume na ninyi ni
wa kwenu" 51 Ikatokea kwamba, kulinga na siku zilivyokua zikikaribia zsiku zake
za kwenda mbinguni, kwa uimara alielekeza uso wake Yerusalemu. 52 Akatuma
wajumbe mbele yake, nao wakaenda na kuingia katika kijiji cha Wasamaria ili
wamtayarishie mahali. 53 Lakini watu huko hawakumpokea, kwasababu alikua
ameelekeza uso wake Yerusalemu. 54 Wanafunzi wake Yakobo na Yohana walipo
liona hili, wakasema, "Bwana unahitaji tuamuru moto ushuke chini kutoka mbinguni
uwateketeze?" 55 Lakini aliwageukia akawakemea. 56 Kisha walikwenda kijiji
kingine. 57 Walipokuwa wakienda katika njia yao, mtu mmoja akamwambia,
"Nitakufuata popote uendapo." 58 Yesu akamwambia, "Mbweha wanamashimo,
ndege wa angani wana viota, lakini mwana wa Adamu hana pakulaza kichwa chake."
59 Ndipo akamwambia mtu mwingine, "Nifuate." Lakini yeye akasema, "Bwana,
niruhusu kwanza niende nikamzika baba yangu," 60 Lakini yeye akamwambia,
"Waache wafu wawazike wafu wao, lakini wewe nenda ukautangaze ufalme wa
Mungu kila mahali." 61 Pia mtu mwingine akasema. "Nitakufuata, Bwana, lakini
niruhusu kwanza nikawaage walio katika nyumba yangu." 62 Laki Yesu akamwambia
hakuna mtu, atiaye mkono wake kulima na kuangalia nyuma atakayefaa kwa ufalme
wa Mungu."

# 10

1 Baada ya mambo hayo, Bwana akachagua sabini wengine, na kuwatuma wawili
wawili wamtangulie katika kila mji na eneo alilotarajia kwenda. 2 Akawaambia,
"Mavuno ni mengi, lakini wafanyakazi ni wachache. Hivyo basi muombeni Bwana
wa mavuno, ili kwamba atume haraka wafanyakazi katika mavuno yake. 3 Enendeni
katika miji. Angalieni, ninawatuma kama kondoo katikati ya mbwa mwitu. 4 Msibebe
mfuko wa pesa, wala mikoba ya wasafiri, wala viatu, wala msimsalimie yeyote njiani.
5 Katika nyumba yeyote mtakayo ingia, kwanza semeni, 'Amani iwe katika nyumba
hii.' 6 kama mtu wa amani yupo pale, amani yenu itabaki juu yake, lakini kama
sivyo, itarudi kwenu. 7 Bakini katika nyumba hiyo, kuleni na mnywe watakachokitoa,
kwa maana mfanyakazi anastahili mshahara wake. Msihame kutoka nyumba hii
kwenda nyingine. 8 Mji wowote muuingiao, na wakawapokea, kuleni chochote
kitakachowekwa mbele yenu, 9 na ponyeni wagonjwa waliomo humo. Semeni kwao,

'Ufalme wa Mungu umekuja karibu yanu' 10 Lakini katika mji wowote mtakaoingia,
na wasiwapokee, nendeni nje katika barabara na semeni, 11 'Hata vumbi katika
mji wenu lililonata miguu mwetu tunalikung'uta dhidi yenu! Lakini tambueni hili,
Ufalme wa Mungu umekaribia.' 12 Ninawambieni kwamba siku ya hukumu itakuwa
ni usitahamilivu zaidi kwa Sodoma kuliko mji huo. 13 Ole kwako Korazini, Ole
kwako Bethsaida! Kama kazi kuu zilizo fanyika ndani yako ingalifanyika Tiro na
Sidoni, Wangelitubu zamani sana, wakikaa ndani ya nguo za gunia na majivu.
14 Lakini itakuwa usitahamilivu zaidi siku ya hukumu kwa Tiro na Sidoni zaidi yenu.
15 Wewe Kapernaumu, Unafikiri utainuliwa mpaka Mbinguni? Hapana, utashushwa
chini mpaka kuzimu 16 Atakaye wasikiliza ninyi anisikiliza mimi, na yeyote atakaye
wakataa anikataa mimi, na yeyote anikataaye mimi anmtakaa aliyenituma" 17 Wale
sabini walirudi kwa furaha, wakisema, "Bwana, hata mapepo wanatutii katika jina
lako." 18 Yesu akawaambia, "Nilimwona Shetani akianguka kutoka mbinguni kama
radi. 19 Tazama, nimewapa mamlaka ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote
za adui, na hapana chochote kwa njia yoyote kitakachowadhuru. 20 Hata hivyo
msifurahi tu katika hili, kwamba roho zinawatii, lakini furahini zaidi kwamba majina
yenu yameandikwa mbinguni." 21 Katika mda uleule alifurahi sana katika Roho
Mtakatifu, na kusema, "Ninakusifu wewe, Baba, Bwana wa mbingu na dunia, kwa
sababu umeyaficha mambo haya kutoka kwa wenye hekima na akili, na kuyafunua
kwa wasio fundishwa, kama watoto wadogo. Ndio, Baba, kwa kuwa ilipendeza
katika machoni pako." 22 "Kila kitu kimekabidhiwa kwangu na Baba yangu, na
hakuna afahamuye Mwana ni nani ila Baba, na hakuna afahamuye Baba ni nani ila
Mwana, na ye yote ambaye Mwana hutamani kujifunua kwake." 23 Akawageukia
wanafunzi, akasema faraghani, "Wamebarikiwa wayaonayo haya ambayo ninyi
mnayaona. 24 Ninawambia ninyi, kwamba manabii wengi na wafalme walitamani
kuona mambo myaonayo, na hawakuyaona, na kusikia kusikia mnayoyaikia, na
hawakuyasikia." 25 Tazama, mwalimu fulani wa sheria ya Kiyahudi alisimama na
kumjaribu, akisema, "Mwalimu, nifanye nini niurithi izima wa milele?" 26 Yesu
akamwambia, "Kimeandikwa nini katika sheria? Unaisoma je?" 27 Akajibu akasema,
"Utampenda Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa
nguvu zako zote, na kwa akili zako zote, na jirani yako kama nafsi yako mwenyewe."
28 Yesu akasema, "Umejibu kwa usahihi. Fanya hivi na utaishi." 29 Lakini mwalimu,
akitamani kujihesabia haki mwenyewe, Akamwambia Yesu, "Na jirani yangu ni
nani?" 30 Yesu akijibu akasema, "Mtu fulani alikuwa akitelemka kutoka Yerusalem
kwenda Yeriko. Akaangukia kati ya wanyang'anyi, waliomnyang'anya mali yake, na
kumpiga na kumuacha karibu akiwa nusu mfu.. 31 Kwa bahati kuhani fulani alikuwa
akishuka katika njia hiyo, alipo muona alipita upande mwingine. 32 Vivyo hivyo
Mlawi pia, alipofika mahali pale na kumuona, akapita upande mwingine. 33 Lakini
Msamaria mmoja, alipokuwa akisafiri, alipita pale alipokuwa mtu huyo. alipomuona,
alisukumwa kwa huruma. 34 Alimkaribia na kumfunga vidonda vyake, akimwiga
mafuta na divai juu yake. Alimpandisha juu ya mnyama wake, na kumpeleka
katika nyumba ya wageni na kumhudumia. 35 Siku ilyofuata alichukua dinari mbili,
na akampatia mmiliki wa nyumba ya wageni na kumwambia, 'Muhudumie na
chochote cha ziada utakacho tumia, nitakulipa nitakaporudi.' 36 Ni yupi kati ya hawa
watatu, unafikiri, alikuwa ni jirani kwake yeye aliyeangukia kati ya wanyang'anyi?"
37 Mwalimu alisema, "Ni yule aliyeonesha huruma kwake." Yesu akamwambia,
"Nenda na ukafanye vivyo hivyo" 38 Sasa walipokuwa wakisafiri, waliingia katika
kijiji fulani, na mwanamke mmoja jina lake Martha alimkaribisha nyumbani kwake.
39 Alikuwa na dada aliyeitwa Mariamu, aliekaa miguuni pa Bwana na kusikiliza neno
lake. 40 Lakini Martha alijipa shughuli nyingi za kuandaa mlo. Alikwenda kwa Yesu,

na kusema, “Bwana, haujali kwamba dada yangu ameniacha nihudumu peke yangu?
Hivyo basi mwambie anisaidie.” 41 Lakini Bwana alimjibu na kumwambia, “Martha,
Martha, una sumbuka juu ya mambo mengi, 42 lakini ni kitu kimoja tu cha muhimu.
Mariamu amechagua kilicho chema, ambacho hakitaondolewa kutoka kwake.”

# 11

1 Ilitokea wakati Yesu alipokuwa anaomba mahali fulani, mmoja wa mwanafunzi
wake alimwambia, “Bwana, tufundishe sisi kuomba kama Yohana alivyo wafundisha
wanafunzi wake'. 2 Yesu akawaambia, Msalipo, semeni, 'Baba, Jina lako litakazwe.
Ufalme wako uje. 3 Utupe mkate wetu wa kila siku. 4 Utusamehe makosa yetu, kama
nasi tunavyowasamehe wote waliotukosea. Usituongoze katika majaribu.” 5 Yesu
akawaambia, “Ni nani kwenu atakuwa na rafiki, ambaye atamuendea usiku, na
kumwambia, Rafiki niazime mikate mitatu. 6 Kwa sababu rafiki yangu amenijia
sasa hivi kutoka safarini, nami sina cha kumuandalia.' 7 Na yule aliyeko ndani
akamjibu, usinitaabishe, Mlango umekwisha kufungwa, na watoto wangu, pamoja
nami tumekwisha kulala kitandani. Siwezi kuamka na kukupa wewe mikate.
8 Nawaambia, japo kuwa haamki na kukupatia mikate kama rafiki yake, kwa sababu
ya kuendelea kumgongea bila aibu, ataamka na kukupatia vipande vingi vya mikate
kulingana na mahitaji yako. 9 Nami pia nawaambieni, Ombeni, nanyi mtapewa;
tafuteni, nanyi mtapata, pigeni hodi nanyi mtafunguliwa. 10 Kwa kuwa kila mtu
aombaye atapokea, na kila mtu atafutaye atapata, na kila mtu apigaye hodi, mlango
utafunguliwa kwake. 11 Ni baba yupi miongoni mwenu, mwanaye akimuomba
samaki atampa nyoka badala yake.? 12 Au akimuomba yai atampa nge badala
yake?. 13 Kwa hiyo, ikiwa ninyi mlio waovu mnajuwa kuwapa watoto wenu zawadi
nzuri, je si zaidi sana Baba yenu wa mbinguni kwamba atawapa Roho Mtakatifu
hao wamuombao?” 14 Baadaye, Yesu akawa anakemea pepo, na mtu mwenye
pepo alikuwa bubu. Ikawa pepo lilipomtoka, mtu huyo aliweza kuongea. Umati
wakastaajabu sana. 15 Lakii watu wengine wakasema, huyu anaondo mapepo kwa
Beelzebul, mkuu wa mapepo 16 Wengine walimjaribu na kumtaka awaonyeshe ishara
kutoka mbinguni. 17 Lakini Yesu aliyatambua mawazo yao na kuwaambia, “Kila
ufalme utakaogawanyika itakuwa ukiwa, na nyumba iliyo gawanyika itaanguka.
18 Kama Shetani atakuwa amegawanyika, ufalme wake utasimamaje? Kwa sababu
mwasema natoa mapepo kwa Belzebuli 19 Kama mimi natoa mapepo kwa Belzebuli,
je wenzenu wanatoa mapepo kwa njia gani? Kwa sababu hii, wao watawahukumu
ninyi. 20 Lakini, kama natoa mapepo kwa kidole cha Mungu, basi uflame wa
Mungu umewajia. 21 Mtu mwenye nguvu aliye na silaha akilinda nyumba yake,
vitu vyake vitakaa salama. 22 Lakini akivamiwa na mtu mwenye nguvu zaidi, Yule
mtu mwenye nguvu atamnyang'anya silaha zake, na kuzichukua mali zake zote.
23 Yeye asiye pamoja nami yuko kinyume nami, na yeye asiyekusanya pamoja nami
hutapanya. 24 Pepo mchafu amtokapo mtu, huenda na kutafuta mahali pasipo na
maji ili ajipumzishe. Atakapokuwa amekosa, husema, 'nitarudi nilipotoka. 25 Akirudi
na kukuta nyumba imefagiliwa na imekaa vizuri. 26 Hivyo huenda na kutafuta
mapepo saba walio waovu kuliko yeye mwenyewe na kuwaleta waje wakae mahali
pale. Na hali ya mtu huyo huwa mbaya kuliko ilivyokuwa mara ya kwanza.”
27 Ilitokea kwamba alipokuwa akisema maneno hayo, mwanamke fulani alipasa sauti
yake zaidi ya wote kwanye mkutano wa watu na kusema “ Limebarikiwa tumbo
lililo kuzaa na matiti uliyoyanyonya” 28 Lakini yeye akasema, wamebarikiwa wale
wasikio neno la Mungu na kulitunza. 29 Wakati umati wa watu wanakusanyika na
kuongezeka, Yesu akaanza kusema “ Kizazi hiki ni kizazi cha uovu. Hutafuta ishara,
na hakuna ishara watayopewa zaidi ya ile ishara ya Yona. 30 Maana kama Yona

alivyokuwa ishara kwa watu wa Ninawi, ndivyo na Mwana wa Adamu atakavyokuwa
ishara kwa kizazi hiki 31 Malkia wa Kusini atasimama siku ya hukumu na watu
wa kizazi hiki na kuwahukumu wao, kwani yeye alitoka katika mwisho wa nchi
ili aje asikilize hekima za Solomoni, na hapa yuko aliye mkuu kuliko Solomoni.
32 Watu wa Ninawi watasimama katika hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki
siku ya hukumu watakihukumu, kwani wao walitubu kwa mahubiri ya Yona, na
tazama, hapa yuko aliye mkuu kuliko Yona. 33 Hakuna Mtu yeyote, awashaye taa na
kuiweka sehemu ya chini yenye giza isiyoonekana au chini ya kikapu, ila huwasha
na kuweka juu ya kitu ili kila mtu aingiaye aweze kuona mwanga. 34 Jicho lako
ni taa ya mwili. Jicho lako likiwa zuri basi mwili wako wote utakuwa kwenye
mwanga. Lakini jicho lako likiwa baya basi mwili wako wote utakuwa kwenye
giza. 35 Kwa hiyo, mjihadhari ili mwanga ulio ndani yenu usitiwe giza. 36 Hivyo
basi, kama mwili wako wote uko kwenye mwanga, na hakuna sehemu iliyo katika
giza, basi mwili wako utakuwa sawa na taa iwakayo na kutoa mwanga kwenu."
37 Alipomaliza kuongea, Farisayo alimwalika akale chakula nyumbani kwake, naye
Yesu akaingia ndani na kuwa pamoja nao. 38 Na Mafarisayo wakashangaa kwa
jinsi ambavyo hakunawa kwanza kabla ya chakula cha jioni. 39 Lakini Bwana
akawaambia, "Ninyi Mafarisayo mnaosha nje ya vikombe na bakuli, lakini ndani
yenu mmejaa tamaa na uovu. 40 Ninyi watu msio na ufahamu, Je yeye aliyeumba
nje hakuumba na ndani pia? 41 Wapeni masikini yaliyo ndani, na mambo yote
yatakuwa safi kwenu. 42 Lakini ole wenu Mafarisayo, kwani mnatoa zaka ya mnanaa
na mchicha na kila aina ya mboga ya bustani. Lakini mmeacha mambo ya haki
na kumpenda Mungu. Ni muhimu zaidi kufanya yaliyo ya haki na kumpenda
Mungu, bila kuacha kufanya na hayo mengine pia. 43 Ole wenu Mafarisayo, kwa
kuwa mnapenda kukaa katika viti vya mbele kwenye masinagogi na kuamkiwa kwa
salamu za heshima sokoni. 44 Ole wenu, kwani mnafanana na makaburi yasiyo
na alama ambayo watu hutembea juu yake pasipokujua." 45 Mwalimu mmoja wa
sheria za Kiyahudi akamjibu na kumwambia, "Mwalimu, unachokisema kinatuudhi
pia sisi." 46 Yesu akasema, "Ole wenu, waalimu wa sheria! kwani mnawapa watu
mizigo mikubwa wasiyoweza kuibeba, walakini ninyi hamgusi mizigo hiyo hata kwa
moja ya vidole vyenu. 47 Ole wenu, kwa sababu mnajenga na kuweka kumbukumbu
kwenye makaburi ya manabii' ambao waliuwawa na mababu zenu. 48 Hivyo ninyi
mwashuhudia na kukubaliana na kazi walizozifanya mababu zenu, kwa sababu
hakika waliwauwa manabii ambao mnajenga kumbukumbu katika makaburi yao.
49 Kwa sababu hiyo pia, hekima ya Mungu inasema, 'Nitawatumia manabii na mitume
nao watawatesa na kuwaua baadhi yao. 50 Kizazi hiki kitawajibika kwa damu ya
manabii waliouawa tangu kuanza kwa dunia, 51 Kutoka damu ya Abeli hadi damu ya
Zakaria, aliyeuawa katikati ya madhabahu na patakatifu. Ndiyo, nawaambia ninyi,
kizazi hiki kitawajibika. 52 Ole wenu waalimu wa sheria za Kiyahudi, kwa sababu
mmechukua funguo za ufahamu; nyie wenyewe hamuingii, na wale wanaotaka
kuingia mnawazuia." 53 Baada ya Yesu kuondoka pale, Waandishi na Mafarisayo
walimpinga na kubishana naye juu ya mambo mengi. 54 wakijaribu kumnsana kwa
maneno yake.

# 12

1 Kwa wakati huo, maelfu mengi ya watu walikusanyika pamoja, kiasi cha kuanza
kukanyagana, akaanza kusema na wanafunzi wake kwanza, "Jihadharini na chachu
ya Mafarisayo ambayo ni unafiki" 2 Na hapatakuwepo na siri iliyofichika ambayo
haitafunuliwa, wala jambo lililofichwa ambalo halitajulikana. 3 Na lolote mlilolisema
katika giza, litasikiwa katika mwanga. Na yoyote mliyoyasema kwenye sikio ndani

ya vyumba vyenu vya ndani vilivyofungwa yatatangazwa juu ya paa la nyumba.
4 Nawaambieni rafiki zangu, msiwaogope wale wauao mwili na kisha hawana
kitu kingine cha kufanya, 5 Lakini nitawaonya mtakaye mwogopa. Mwogopeni
yule ambaye baada ya kuwa ameua, ana mamlaka ya kutupa jehanamu. Ndiyo,
nawaambiani ninyi, mwogopeni huyo. 6 Je shomoro watano hawauzwi kwa sarafu
mbili? hata hivyo hakuna hata mmoja wao atakayesahaulika mbele za Mungu.
7 Lakini mjue kuwa, nywele za vichwa vyenu vimehesabiwa. Msiogope. Ninyi ni
wa thamani kubwa kuliko shomoro wengi. 8 Ninawaambia, yeyote atakayenikiri
Mimi mbele za watu, Mwana wa Adamu atamkiri mbele za malaika wa Mungu.
9 Lakini yeyeyote atakayenikana mbele za watu naye atakanwa mbele ya Malaika wa
Mungu. 10 Yeyote atakayesema neno baya juu ya Mwana wa Adamu, atasamehewa,
lakini yeyote atakayemkufuru Roho Mtakatifu, hatasamehewa. 11 Watakapowapeleka
mbele za wakuu wa masinagogi, watawala, na wanye mamlaka, msiogope juu na
namna ya kuongea katika kujitetea au nini mtakachosema, 12 kwa kuwa Roho
Mtakatifu atawafundisha namna mtakavyosema kwa wakati huo." 13 Mtu mmoja
katika kusanyiko akamwambia, "Mwalimu, mwambie ndugu yangu anigawie sehemu
ya uruthi wangu." 14 Yesu akamjibu, ni nani aliye niweka kuwa mwamuzi na
mpatanishi kati yenu.? 15 Ndipo akawaambia, Jihadharini na kila namna ya tamaa,
kwa sababu uzima wa mtu hauko katika wingi wa vitu alivyo navyo." 16 Yesu
akawaambia mfano, akisema, Shamba la mtu mmoja tajiri lilizaa sana, 17 na
akajiuliza ndani yake, akisema, nitafanyaje kwani sina mahali pa kuhifadhi mazao
yangu? 18 Akasema, nitafanya hivi. Nitavunja ghala zangu ndogo na kujenga iliyo
kubwa, na kuyahifadhi mazao yangu yote na vitu vingine. 19 Nitaiambia nafsi
yangu, "Nafsi, umejiwekea akiba ya vitu vingi kwa miaka mingi. Pumzika, ule,
unywe na kustarehe." 20 Lakini Mungu akamwambia, ewe mtu mpumbavu, usiku
wa leo wanahitaji roho kutoka kwako, na vitu vyote ulivyoviandaa vitakuwa vya
nini? 21 Ndivyo itakavyokuwa kwa kila mtu anayejiwekea mali na si kujitajirisha
kwa ajili ya Bwana. 22 Yesu akawaambia wanafunzi wake, Kwa hiyo nawaambia
msihofu juu ya maisha yenu__ya kuwa mtakula nini au juu ya miili yenu __ya kuwa
mtavaa nini 23 Kwa kuwa maisha ni zaidi ya chakula, na mwili ni zaidi ya mavazi.
24 Angalieni ndege wa angani, hawalimi wala hawavuni. Hawana chumba wala ghala
ya kuhifadhia, lakini Baba yenu huwalisha. Ninyi si bora zaidi kuliko ndege! 25 Ni
yupi kati yenu ambaye akijisumbua ataweza kuongeza dhiraa moja katika maisha
yake? 26 Ikiwa basi hamuwezi kufanya hicho kitu kidogo kilicho rahisi kwa nini basi
kusumbukia hayo mengine?. 27 Angalieni maua -yanavyomea. Hayafanyi kazi wala
hayasokoti. Lakini nawaambia, hata Sulemani katika utukufu wake wote hakuvikwa
kama mojawapo ya haya, 28 Kama Mungu huyavika vizuri majani ya kondeni, ambayo
leo yapo, na kesho hutupwa kwenye moto. Je si zaidi atawavika ninyi? enyi wa imani
haba! 29 Msisumbukie juu ya kuwa mtakula nini au mtakunywa nini, wala msiwe
na hofu. 30 Kwa kuwa Mataifa yote ya dunia husumbukia mambao yao. Na Baba
yenu anajua ya kuwa mnahitaji hayo. 31 Lakini tafuteni ufalme wake kwanza, na
hayo mengine mtazidishiwa, 32 msiogope, enyi kundi dogo, kwa sababu Baba yenu
anafurahia kuwapa ninyi huo ufalme. 33 Uzeni mali zenu na mkawape maskini,
mjifanyie mifuko isiyoishiwa__hazina ya mbinguni isiyokoma, sehemu ambapo wezi
hawatakaribia wala nondo haitaweza kuharibu. 34 Kwa kuwa palipo na hazina yako,
ndipo na roho yako itakapokuwepo. 35 Nguo zenu ndefu ziwe zimefungwa kwa
mkanda, na taa zenu zihakikishwe kuwa zinaendelee kuwaka, 36 na muwe kama
watu wanaomtazamia Bwana wao kutoka kwenye sherehe ya harusi, ili kwamba
akija na kupiga hodi, wataweze kumfungulia mlango kwa haraka. 37 Wamebarikiwa
wale watumishi, ambao Bwana atawakuta wako macho. Hakika atafunga nguo yake

ndefu kwa mkanda, kisha atawaketisha chini kwa chakula, na kisha kuwahudumia.
38 Kama Bwana atakuja kwa zamu ya pili ya ulinzi ya usiku, au hata zamu ya tatu ya
ulinzi, na kuwakuta wakiwa tayari, itakuwa ni heri kwa hao watumishi. 39 Zaidi ya
hayo, mjue hili, kama bwana mwenye nyumba angelijua saa ambayo mwivi anakuja,
asingeliruhusu nyumba yake ifunjwe. 40 Iweni tayari pia kwani hamjui ni wakati
gani mwana wa Adamu atarudi. 41 Petro akasema, "Bwana, watuambia sisi wenyewe
hii mifano, au unamwambia kila mtu.? 42 Bwana akawaambia, "Ni nani mtumwa
mwaminifu au mwenye hekima ambaye bwana wake atamweka juu ya watumishi
wengine, ili awagawie chakula chao kwa wakati mwafaka? 43 Amebarikiwa mtumishi
yule, ambaye bwana wake akija atamkuta akifanya yale aliyoagizwa. 44 Hakika
nawaambia ninyi ya kuwa atamweka juu ya mali yake yote. 45 Lakini Mtumishi
yule akisema moyoni mwake, "bwana wangu anachelewa kurudi; hivyo akaanza
kuwapiga wale watumishi wa kiume na wa kike, kisha akaanza kula, kunywa na
kulewa, 46 bwana wake yule mtumwa atakuja katika siku asiyotegemea na saa
asiyoijua, naye atamkata vipande vipande na kumuweka katika sehemu pamoja
na wasiokuwawaaminifu' 47 Mtumishi, anayejua mapenzi ya bwana wake, naye
hakujiandaaa wala hakufanya sawa sawa na mapenzi yake, atapigwa viboko vingi.
48 Lakini mtumishi asiyejua mapenzi ya bwana wake, lakini akafanya yanayostahili
adhabu, atapigwa viboko vichache. Kwa kuwa yeye aliyepewa vingi, vingi hudaiwa
kutoka kwake, na yeye aliyeaminiwa kwa vingi, kwake vitadaiwa vingi zaidi.
49 Nimekuja kuwasha moto duniani, na natamani iwe umekwishawaka, 50 Lakini
nina ubatizo ambao nitabatizwa, na nina huzuni mpaka utkapokamilika! 51 Je
mnafikiri kuwa nimekuja kuleta amani duniani? Hapana, Nawaambieni, badala
yake nimeleta mgawanyiko. 52 Tangu sasa na kuendelea kutakuwa na watu watano
katika nyumba moja wamegawanyika, na watatu watakuwa kinyume na wawili, na
wawili watakuwa kinyume na watatu. 53 Watagawanyika, baba atakuwa kinyume
na mwanae, na mwanae atakuwa kinyume na babaye, mama atakuwa kinyume
na binti yake, na binti atakuwa kinyume na mama yake, Mama mkwe atakuwa
kinyume na mkwe wake naye mkwe atakuwa kinyume na mama mkwe wake. 54 Yesu
akawa anawaambia makutano pia, "Mara muonapo mawingu yakitokea magharibi,
mnasema nyakati za mvua zimewadia; na ndivyo inavyo kuwa, 55 Na upepo
wa kusini ukivuma, mnasema, Patakuwepo na joto kali, na ndivyo inavyokuwa.
56 Enyi wanafiki, mnaweza kutafsiri mwonekano wa nchi na anga, lakini inakuwaje
hamuwezi kuutafsiri wakati uliopo? 57 Ni kwa nini kila mmoja wenu asipambanue
lililo sahihi kwake kulifanya wakati ambapo angali na nafasi ya kufanya hivyo?
58 Maana mkienda na mshitaki wako mbele ya hakimu, jitahidi kupatana na mshitaki
wako mungali bado mko njiani asije akakupeleka kwa hakimu, na hakimu akupeleka
kwa ofisa, na ofisa akakutupa gerezani. 59 Nakuambia, hutatoka huko hadi umelipa
mpaka senti ya mwisho.

# 13

1 Kwa wakataihuo huo, kulikuwa na baadhi watu waliomtaarifu juu ya Wagalilaya
ambao Pilato aliwaua na kuchanganya damu yao na sadaka zao. 2 Yesu akajibu
na kuwaambia, "Je mwadhani kuwa Wagalilaya hao walikuwa na dhambi kuliko
Wagalilaya wengine wote ndiyo maana wamepatwa na mabaya hayo? 3 Hapana,
nawaambia, lakini msipotubu, nanyi mtaangamia vivyo hivyo. 4 Au wale watu kumi
na nane katika Siloamu ambao mnara ulianguka na kuwaua, mnafikiri wao walikuwa
wenye dhambi zaidi kuliko watu wengine katika Yerusalemu? 5 Hapana, mimi
nasema, lakini kama msipotubu, ninyi nyote pia mtaangamia. 6 Yesu aliwaambia
mfano huu, "Mtu mmoja alikuwa na mtini umepandwa katika shamba lake na

alikwenda kutafuta matunda juu yake lakini hakupata. 7 Akamwambia mtunza
bustani, 'Tazama, kwa miaka mitatu nimekuja na kujaribu kutafuta matunda kwenye
mtini huu lakini sikupata. Uukate. Kwani ulete uharibifu wa ardhi? 8 Mtunza
bustani akajibu na kusema, 'uache mwaka huu ili niupalilie na kuweka mbolea juu
yake. 9 Kama ukizaa matunda mwaka ujao, ni vema; lakini kama hautazaa, uukate.!”'
10 Sasa Yesu alikuwa akifundisha katika mojawapo ya Masinagogi wakati wa Sabato.
11 Tazama, alikuwepo mama mmoja ambaye kwa miaka kumi na minane alikuwa
na rohomchafu wa udhaifu, na yeye alikuwa amepinda na hana uwezo kabisa
wa kusimama. 12 Yesu alipomwona, alimwita, akamwambia, “Mama, umewekwa
huru kutoka kwenye udhaifu wako.” 13 Akaweka mikono yake juu yake, na mara
mwili wake akajinyoosha na akamtukuza Mungu. 14 Lakini mkuu wa sinagogi
alikasirika kwa sababu Yesu alikuwa amemponya siku ya Sabato. Hivyo mtawala
akajibu akawambia makutano, “Kuna siku sita ambazo ni lazima kufanya kazi.
Njoni kuponywa basi, si katika siku ya Sabato. ' 15 Bwana akamjibu na akasema,
“wanafiki! Hakuna kila mmoja wenu kufungua punda wako au ng'ombe kutoka zizini
na kuwaongoza kumpeleka kunywa siku ya Sabato? 16 Hivyo pia binti wa Abrahamu,
ambaye Shetani amemfunga kwa miaka kumi na minane, je haikumpasa kifungo
chake kisifunguliwe siku ya sabato?” 17 Alipokuwa akisema maneno hayo, wale wote
waliompinga waliona aibu, bali makutano wote wa wengine walishangilia kwa ajili
ya mambo ya ajabu aliyotenda. 18 Yesu akasema, “Ufalme wa Mungu unafanana na
nini, na naweza kuulinganisha na nini? 19 Ni kama mbegu ya haradari aliyoitwaa mtu
mmoja na kuipanda shambani mwake, na ikamea ikawa mti mkubwa, na ndege wa
mbinguni wakajenga viota vyao katika matawi yake. 20 Tena akasema, “Niufananishe
na nini ufalme wa Mungu? 21 Ni kama chachu ambayo mwanamke aliichukua na
kuchanganyakwenye vipimo vitatu vya unga hata ukaumuka.” 22 Yesu alitembelea
kila mji na kijiji njiani akielekea Yerusalemu na kuwafundisha. 23 Mtu mmoja
akauliza, “Bwana, ni watu wachache tu watakaookolewa?” Hivyo akawaambia,
24 “Jitahidi kuingia kwa kupitia mlango mwembamba, kwa sababu wengi watajaribu
na hawataweza kuingia. 25 Mara baada ya mmiliki wa nyumba kusimama na
kufunga mlango, basi mtasimama nje na kupiga hodi mlangoni na kusema, Bwana,
Bwana, tufungulie yeye atajibu na kuwaambia, siwajui ninyi wala mtokako.' 26 Ndipo
mtasema, Tulikula na kunywa mbele yako na wewe ulifundisha katika mitaa yetu.”
27 Lakini yeye atawajibu, `nawaambia, siwajui mtokako, ondokeni kwangu, ninyi
watenda maovu!' 28 Kutakuwa na kilio na kusaga meno wakati mtakapowaona
Abrahamu, Isaka, Yakobo na manabii wote katika ufalme wa Mungu, lakini ninyi
wenyewe mumetupwa nje. 29 Watafika kutoka Mashariki, Magharibi, Kaskazini na
Kusini, na kupumzika katika meza ya chakula cha jioni katika ufalme wa Mungu.
30 Na tambua hili, wa mwisho ni wa kwanza na wa kwanza atakuwa wa mwisho.”
31 Muda mfupi baadaye, baadhi ya Mafarisayo walikuja na kumwambia, “Nenda
na ondoka hapa kwa sababu Herode anataka kukuua.” 32 Yesu akasema, “Nendeni
mkamwambie yule mbweha, `Tazama, ninawafukuza pepo na kufanya uponyaji leo
na kesho, na siku ya tatu nitatimiza lengo langu. 33 Katika hali yoyote, ni muhimu
kwa ajili yangu kuendelea leo, kesho, na siku iliyofuata, kwa vile haikubaliki kumuua
nabii mbali na Yerusalemu. 34 Yerusalemu, Yerusalemu, nani anawaua manabii
na kuwapiga mawe wale waliotumwa kwenu. Mara ngapi nimetaka kuwakusanya
watoto wenu kama vile kuku anavyokusanya vifaranga vyake chini ya mbawa zake,
lakini humkulitaka hili. 35 Tazama, nyumba yako imetelekezwa. Nami nawaambia,
hamuwezi kuniona hata mtakaposema 'Amebarikiwa huyo ajaye kwa jina la Bwana.'”

# 14

1 Iltokea siku ya Sabato, alipokua akienda nyumbani kwa mmoja wa viongozi
wa Mafarisayo kula mkate, nao walikuwa wakimchunguza kwa karibu. 2 Tazama,
pale mbele yake alikuwa mtu ambaye anasumbuliwa na uvimbe. 3 Yesu aliuliza
wataalam katika sheria ya Wayahudi na Mafarisayo, “Je, ni halali kumponya siku
ya Sabato, au sivyo?” 4 Lakini wao walikuwa kimya, kwahiyo Yesu akamshika,
akamponya na kumruhusu aende zake. 5 Naye akawaambia, “Ni nani kati yenu
ambaye ana mtoto au ng'ombe anatumbukia kisimani siku ya Sabato hata mvuta
nje mara moja?” 6 Wao hawakuwa na uwezo wa kutoa jibu kwa mambo haya.
7 Wakati Yesu alipogundua jinsi wale walioalikwa kwamba wamechagua viti vya
heshima, akawaambia mfano, akiwaambia, 8 “Wakati mnapoalikwa na mtu harusini,
usiketi katika nafasi za heshima, kwa sababu inawezekana amealikwa mtu ambaye ni
wakuheshimiwa zaidi kuliko wewe. 9 Wakati mtu aliyewaalika ninyi wawili akifika,
atakuambia wewe, “mpishe mtu huyu nafasi yako,” na kisha kwa aibu utaanza
kuchukua nafasi ya mwisho. 10 Lakini wewe ukialikwa, nenda ukakae mahali pa
mwisho, ili wakati yule aliyekualika akija, aweze kukuambia wewe, `Rafiki, nenda
mbele zaidi.” ndipo utakuwa umeheshimika mbele ya wote walioketi pamoja nawe
mezani. 11 Kwa maana kila ajikwezaye atashushwa, na yeye ajishushae atakwezwa.
' 12 Yesu pia alimwambia mtu aliyemwalika, 'Unapotoa chakula cha mchana au
cha jioni, usiwaalike rafiki zako au ndugu zako au jamaa zako au majirani zako
matajiri, ili kwamba wao wasije wakakualika wewe ukapata malipo. 13 Badala
yake, unapofanya sherehe, waalike maskini, vilema, viwete na vipofu, 14 na wewe
utabarikiwa, kwa sababu hawawezi kukulipa. Kwa maana utalipwa katika ufufuo
wa wenye haki.” 15 Wakati mmoja wa wale walioketi mezani pamoja na Yesu
aliposikia hayo, naye akamwambia, “Amebarikiwe yule atakayekula mkate katika
Ufalme wa Mungu!” 16 Lakini Yesu akamwambia, “Mtu mmoja aliandaa sherehe
kubwa, akaalika watu wengi. 17 Wakati sherehe ilipokuwa tayari, alimtuma mtumishi
wake kuwaambia wale walioalikwa, `'Njooni, kwa sababu vitu vyote vimekwisha
kuwekwa tayari.' 18 Wote, wakaanza kuomba radhi. Wa kwanza akamwambia
mtumishi, 'Nimenunua shamba, lazima niende kuliona. Tafadhali unisamehe.' 19 Na
mwingine akasema, `'Nimenunua jozi tano za ng'ombe, na mimi naenda kuwajaribu.
Tafadhali uniwie radhi.' 20 Na mtu mwingine akasema, 'Nimeoa mke, kwa hiyo
siwezi kuja.' 21 Mtumishi akarudi na kumwambia bwana wake mambo hayo. Yule
mwenye nyumba alikasirika akamwambia mtumishi wake, `'Nenda upesi mitaani na
katika vichochoro vya mji ukawalete hapa maskini, vilema, vipofu na walemavu.”
22 Mtumimishi akasema, `Bwana, hayo uliyoagiza yamekwisha tendeka, na hata sasa
bado kuna nafasi.' 23 Bwana akamwambia mtumishi, 'Nenda katika njia kuu na
vichochoro na uwashurutishe watu waingie, ili nyumba yangu ijae. 24 Kwamaana
nawaambia, katika wale walioalikwa wa kwanza hapana atakayeonja sherehe yangu.
' 25 Sasa umati mkubwa walikuwa wanakwenda pamoja naye, naye akageuka na
akawaambia, 26 'Kama mtu akija kwangu naye hamchukii baba yake, mama yake,
mke wake, watoto wake, ndugu zake waume na wanawake- ndio, na hata maisha yake
pia -hawezi kuwa mwanafunzi wangu. 27 Mtu asipochukua msalaba wake na kuja
nyuma yangu hawezi kuwa mwanafunzi wangu. 28 Maana ni nani kati yenu, ambaye
anatamani kujenga mnara hataketi kwanza akadirie gharama kwa mahesabu kama
ana kile anachohitaji ili kukamilisha hilo? 29 Vinginevyo, baada ya kuweka msingi
na kushindwa kumaliza, wote walioona wataanza kumdhihaki, 30 wakisema, Mtu
huyu alianza kujenga, akawa hana nguvu za kumaliza.' 31 Au mfalme gani, akitaka
kwenda kupigana na mfalme mwingine katika vita, ambae hatakaa chini kwanza
na kuchukua ushauri kuhusu kama ataweza, pamoja na watu elfu kumi kupigana

na mfalme mwingine anayekuja juu yake na watu elfu ishirini? [32] Na kama sivyo,
wakati jeshi la wengine bado liko mbali, hutuma balozi kutaka masharti ya amani.
[33] Kwa hiyo basi, yeyote kati yenu ambaye hataacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa
mwanafunzi wangu. [34] Chumvi ni nzuri, lakini ikiwa Chumvi imepoteza ladha yake,
jinsi gani inaweza kuwa chumvi tena? [35] Haina matumizi kwa udongo au hata kwa
mbolea. hutupwa mbali. Yeye aliye na masikio ya kusikia, na asikie."

# 15

[1] Basi watoza ushuru wote na wengine wenye dhambi walikuja kwa Yesu na
kumsikiliza. [2] Mafarisayowaote na waandishi wakanung'unika wakisema, "Mtu huyu
huwakaribisha wenye dhambi na hata hula nao." [3] Yesu akasema mfano huu kwao,
akisema [4] "Nani kwenu, kama ana kondoo mia moja na akipotelewa na mmoja wao,
hatawaacha wale tisini na tisa nyikani, na aende akamtafute yule aliyepotea hadi
amwone? [5] Naye akisha kumpata humweka mabegani pake na kufurahia. [6] Afikapo
kwenye nyumba, huwaita rafiki zake na jirani zake akawaambia furahini pamoja
nami, kwa kuwa nimempata kondoo wangu aliyepotea.' [7] nawaambia vivyo hivyo
kutakuwa na furaha mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye, zaidi
ya wenye haki tisini na tisa ambao hawana haja ya kutubu [8] Au kuna mwanamke
gani mwenye sarafu kumi za fedha, akipotewa na sarafua moja, hata washa taa
na kufagia nyumba na kutafuta kwa bidii hadi atakapoipata? [9] Na akiisha kuiona
huwaita rafiki zake na jirani zake akawaambia furahini pamoja nami, kwa kuwa
nimeipata tena sarafu yangu niliyokua nimeipoteza. [10] Hata hivyo nawaambia kuna
furaha mbele ya malaika wa Mungu kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja atubuye."
[11] Na Yesu akasema, "Mtu mmoja alikua na wana wawili [12] yule mdogo akamwambia
babaye, Baba nipe sehemu ya mali inayonistali kuirithi. Hivyo akagawanya mali
zake kati yao. [13] Siku si nyingi yule mdogo akakusanya vyote anavyomiliki akaenda
nchi ya mbali, na huko akatapanya hela zake, kwa kununua vitu asivyo vihitaji, na
kutapanya fedha zake kwa anasa. [14] Nae alipokua amekwisha tumia vyote njaa
kuu iliingia nchi ile naye akaanza kuwa katika uhitaji. [15] Akaenda na kujiajiri
mwenyewe kwa mmoja wa raia wa nchi ile, naye alimpeleka shambani kwake
kulisha nguruwe. [16] Na akawa akitamani kujishibisha kwa maganda waliyokula
nguruwe kwa sababu hakuna mtu aliempa kitu chochote apate kula. [17] Ila yule
mwana mdogo alipozingatia moyoni mwake, alisema 'ni watumishi wangapi wa
baba yangu wanachakula kingi cha kutosha na mimi niko hapa, ninakufa na njaa!
[18] Nitaondoka na kwenda kwa baba yangu, na kumwambia, "Baba nimekosa juu ya
mbingu na mbele ya macho yako. [19] Sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye
kama mmoja wa watumishi wako." [20] Ndipo akaondoka akaenda kwa baba yake.
Alipokua angali mbali baba yake alimuona akamwonea huruma akaenda mbio na
kumkumbatia na kumbusu. [21] Yule mwana akamwambia, 'baba nimekosa juu ya
mbingu na mbele ya macho yako sistahili kuitwa mwana wako.' [22] Yule baba
aliwaambia watumishi wake, 'lileteni upesi vazi lililo bora, mkamvike mtieni na pete
kidoleni na viatu miguuni. [23] Kisha mleteni ndama yule alienona mkamchinje tule
na kufurai. [24] Kwa kuwa mwanangu alikua amekufa naye yu hai. Alikua amepotea
nae ameonekana wakaanza kushangilia. [25] Basi yule mwanae mkubwa alikuwako
shamba. Alipokuwa akija na kuikaribia nyumba alisikia sauti ya nyimbo na michezo.
[26] Akaita mtumishi mmoja akamuuliza mambo haya maana yake nini? [27] Mtumishi
akamwambia mdogo wako amekuja na baba yako amemchinjia ndama aliyenona
kwa sababu amerudi salama.' [28] Mwana mkubwa akakasirika akakataa kuingia ndani
na babaye alitoka nje kumsihi. [29] Ila akamjibu babayake akisema, 'Tazama mimi
nimekutumikia miaka mingi, wala sijakosa amri yako, lakini hujanipa mwana mbuzi,

ili niweze kusherehekea na rafiki zangu. [30] Lakini alipokuja huyu mwana wako
aliyetapanya mali yako yote pamoja na makahaba umemchinjia ndama alienona.
[31] Baba akamwambia, 'Mwanangu, wewe u pamoja nami siku zote na vyote nilivyo
navyo ni vyako. [32] Ila ilikua vyema kwetu kufanya sherehe na kufurahi, huyu ndugu
yako alikua amekufa, na sasa yu hai; alikua amepotea naye ameonekana."

# 16

[1] Yesu aliwaambia tena wanafunzi wake, "Palikuwa na mtu mmoja tajiri aliyekuwa
na meneja, na alitaarifiwa ya kwamba meneja huyu anatapanya mali zake. [2] Hivyo
tajiri akamwita, akamwambia, "Ni nini hii ninayo isikia juu yako? Toa hesabu
ya umeneja wako, kwa kuwa huwezi kuwa meneja tena.' [3] Yule meneja akasema
moyoni mwake, Nifanye nini, maana bwana wangu ananiondolea kazi yangu ya
umeneja? Sina nguvu za kulima, na kuomba naona haya. [4] Najua nitakalotenda ili
nitakapotolewa katika kazi yangu ya uwakili watu wanikaribishe nyumbani mwao.
[5] Hivyo wakili akawaita wadeni wa bwana wake kila mmoja akamwambia wa
kwanza, 'unadaiwa kiasi gani na bwana wangu?' [6] Akasema vipimo mia moja
vya mafuta akamwambia 'chukua hati yako keti upesi andika hamsini.' [7] kisha
akamwambia mwingine na wewe unadaiwa kiasi gani?' akasema 'vipimo mia
moja vya unga vya ngano.' Akamwambia 'twaa hati yako andika themanini.'
[8] Yule bwana akamsifu meneja dhalimu kwa vile alivyotenda kwa wereu. Kwakua
watoto wa ulimwengu huu ni werevu nyingi na hushughulika kwa ujanja na watu
wa upande wao kuliko walivyo watoto wa nuru. [9] Nami nawaambia jifanyieni
marafiki kwa mali ya udhalimu ili itakapokosekana wawakaribishe katika makao
ya milele. [10] Aliye mwaminifu katika lililo dogo sana huwa mwaminifu katika
lililo kubwa pia. na aliye dhalimu katika lililo dogo huwa dhalimu katika lililo
kubwa pia. [11] Kama ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu ni nani
atakayewaamini katika mali ya kweli? [12] Na kama hamkuwa waaminifu katika
kutumia mali ya mtu mwingine ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe? [13] Hakuna
mtumishi awezaye kutumikia mabwana wawili, kwamaana atamchukia mmoja na
kumpenda mwingine, ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu. Hamuwezi
kumtumikia Mungu na mali." [14] Basi Mafarisayo, ambao walikuwa wanapenda
fedha waliyasikia haya yote na wakamdhihaki. [15] Na akawaambia, "Ninyi ndiyo
mnaojidai haki mbele ya wanadamu, lakini Mungu anaijua mioyo yenu. Kwa kuwa
lililotukuka kwa wanadamu huwa chukizo mbele za Mungu. [16] Sheria na manabii
vilikuwapo mpaka Yohana alivyokuja. Tangu wakati huo, habari njema ya ufalme
wa Mungu hutangazwa, na kila mtu hujaribu kujiingiza kwa nguvu. [17] Lakini ni
rahisi kwa mbingu na nchi vitoweke kuliko hata herufi moja ya sheria ikosekane.
[18] Kila amwachaye mkewe na kumwoa mke mwingine azini, naye amwooaye yeye
aliyeachwa na mumewe azini. [19] Palikua na mtu mmoja tajiri aliyevaa nguo
za rangi ya zambarau na kitani safi na alikua akifurahia kila siku utajiri wake
mkubwa. [20] Na maskini mmoja jina lake Lazaro aliwekwa getini pake, na ana
vidonda. [21] Naye alikua akitamani kushibishwa kwa makombo yaliyoanguka katika
meza ya yule tajiri hata mbwa wakaja wakamlamba vidonda vyake. [22] Ikawa yule
maskini alikufa na akachukuliwa na Malaika mpaka kifuani kwa Ibrahimu. Yule
tajiri naye akafa akazikwa. [23] Na kule kuzimu alipokua katika mateso aliyainua
macho yake akamuona Ibrahimu kwa mbali na Lazaro kifuani mwake. [24] Akalia
akasema, 'Baba Ibrahimu, nihurumue umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake
majini, auburudishe ulimi wangu; kwa sababu ninateswa katika moto huu. [25] Lakini
Ibrahimu akasema, 'Mwanangu kumbuka ya kwamba katika maisha yako uliyapokea
mambo yako mema, na Lazaro vivyo alipata mabaya. Ila sasa yupo hapa anafarijiwa

na wewe unaumizwa. 26 Na zaidi ya hayo, kumewekwa shimo kubwa na refu
kati yetu, ili wale wanaotaka kutoka huku kwenda kwenu wasiweze wala watu wa
kwenu wasivuke kuja kwetu.' 27 Yule tajiri akasema, 'Nakuomba Baba Ibrahimu,
kwamba umtume nyumbani kwa baba yangu 28 kwa kuwa ninao ndugu watano ili
awaonye, kwa hofu kwamba wao pia watkuja mahali hapa pa mateso. ' 29 Lakini
Ibrahimu akasema, 'Wanao Musa na manabii. Waache wawasikilize wao. 30 Yule
tajiri akasema, 'hapana, Baba Ibrahimu, lakini kama akiwaendea mtu atokaye kwa
wafu watatubu.' 31 Lakini Ibrahimu akamwambia, 'wasipowasikia Musa na manabii
hawatashawishiwa hata mtu akifufuka katika wafu.

# 17

1 Yesu akawaambia wanafunzi wake, “mambo yasababishayo watu watende
dhambi hayana budi kutokea, Lakini ole wake mtu anayeyasababisha! 2 Ingekua ni
heri kama mtu huyo angefungiwa jiwe zito la kusagia shingoni na kutubwa baharini,
kuliko kumfanya mmoja wa hawa wadogo atende dhambi. 3 Jilindeni. Kama ndugu
yako akikukosea mwonye, naye akitubu msamehe. 4 Kama akikukosea mara saba
kwa siku moja na mara saba kwa siku moja akaja kwako akisema, 'ninatubu,'
msamehe!” 5 Mitume wake wakamwambia Bwana, “tuongezee imani yetu.” 6 Bwana
akasema, “kama mgekuwa na imani kama punje ya haradarii, mngeweza kuuambia
mti huu wa mkuyu, 'n'goka na ukaote baharini,' nao ungewatii. 7 Lakini nani
miongoni mwenu, ambaye ana mtumishi anayelima shamba au anayechunga kondoo,
atamwambia arudipo shambani, 'Njoo haraka na keti ule chakula? 8 Je hatamwambia,
'Niandalie chakula nile, na jifunge mkanda na unitumikie mpaka nitakapo maliza
kula na kunywa. Baada ya hapo uta kula na kunywa? 9 Hata mshukuru mtumishi
huyo kwasababu katimiza yale aliyoamriwa? 10 Vivyo hivyo nanyi mkiisha kufanya
mliyoagizwa semeni 'Sisi tu watumishi tusiostahili. Tumefanya tu yale tuliyopaswa
kufanya.' 11 Ilitokea kwamba alivyokua akisafiri kwenda Yerusalemu, alipita
mpakani mwa Samaria na Galilaya. 12 Alipokua akiingia kwenye kijiji kimoja, huko
alikutana na watu kumi waliokuwa na ukoma. Wakasimama mbali 13 wakapaza
sauti wakasema “Yesu, Bwana tuhurumie.” 14 Alipowaona akawaambia, “Nendeni
mkajionyeshe kwa makuhani.” nao walipokua wakienda wakatakasika. 15 Mmoja
wao alipoona kwamba amepona, akarudi kwa sauti kuu akimsifu Mungu. 16 Akapiga
magoti miguuni mwa Yesu akamshukuru. Yeye alikua msamaria. 17 Yesu akajibu,
akasema, “Je hawakutakasika wote kumi? Wako wapi wale wengine tisa? 18 Hakuna
hata mmoja aliyeonekana kurudi ili kumtukuza Mungu, isipokuwa huyu mgeni?”
19 Akamwambia, “Inuka na uende zako imani yako imekuponya.” 20 Alipoulizwa
na mafarisayo ufalme wa Mungu utakuja lini, Yesu akawajibu akisema, “Ufalme wa
Mungu sio kitu ambacho kinaweza kuonekana. 21 Wala watu hawatasema, 'Angalia
hapa!' au, 'Angalia kule!' kwa maana ufalme wa Mungu umo ndani yenu.” 22 Yesu
akawaambia wanafunzi wake, “Wakati utafika ambapo mtatamani kuiona moja ya
siku ya Mwana wa Adamu, lakini hamtaiona. 23 Watawaambia, 'Angalia, kule!
Angalia, hapa!' Lakini msiende kuangalia, wala kuwafuafata, 24 kama umeme wa radi
umulikao katika anga kuanzia upande mmoja hadi mwingine. Hivyo hata Mwana wa
Adamu atakuwa ivyo katika siku yake. 25 Lakini kwanza itampasa kuteseka katika
mambo mengi na kukataliwa na kizazi hiki. 26 Kama ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo
itakavyokua katika siku ya Mwana wa Adam. 27 Walikula, walikunywa, wakioa na
kuolewa mpaka siku ile ambayo Nuhu alipoingia katika safina na gharika ikaja na
kuwaangamiza wote. 28 Ndivyo ilivyokua katika siku za Lutu, walikula, kunywa,
wakinunua na kuuza, kulima na walijenga. 29 Lakini siku ile Lutu alipoondoka
Sodoma, ikanyesha mvua ya moto na kiberiti kutoka mbinguni ikawaangamiza wote.

30 Hivyo ndivyo itakavyo kuwa siku ile ya Mwana wa Adamu atakapofunuliwa. 31 Siku
hiyo, usimruhusu aliye kwenye dari ya nyumba ashuke kuchukue bidhaa zake ndani
ya nyumba. Na usimruhusu aliyeko shambani kurudi nyumbani. 32 Mkumbuke
mke wa Lutu. 33 Ye yote anaejaribu kuyaokoa maisha yake atayapoteza, lakini ye
yote atakayeyapoteza maisha yake atayaokoa. 34 Nakwambia, usiku huo kutakua na
watu wawili katika kitanda kimoja. Mmoja atachukuliwa, na mwingine ataachwa.
35 Kutakua na wanawake wawili wanasaga nafaka pamoja, mmoja atachukuliwa na
mwingine ataachwa.” 37 Wakamwuliza, “Wapi, Mungu?” Akawaambia, “Pale ulipo
mzoga, ndipo tai hukusanyika kwa pamoja.”

# 18

1 Kisha akawaambia mfano wa namna wanavyopaswa kuomba daima, na wasikate
tamaa. 2 akaisema, 'Kulikuwa na hakimu katika mji fulani, ambaye hakuwa
anamwogopa Mungu na hakuwaheshimu watu. 3 Kulikuwa na mjane katika jiji hilo,
naye alimwendea mara nyingi, akisema, 'Nisaidie kupata haki dhidi ya mpinzani
wangu.' 4 Kwa muda mrefu hakuwa tayari kumsaidia, lakini baada ya muda akasema
moyoni mwake, `Ingawa mimi simwogopi Mungu au kuheshimu mtu, 5 lakini kwa vile
huyu mjane ananisumbua nitamsaidia kupata haki yake, ili asije akanichosha kwa
kunijia mara kwa mara. '' 6 Kisha Bwana akasema, 'Sikiliza alivyosema huyo hakimu
dhalimu. 7 Je Mungu pia hataleta haki kwa wateule wake ambao wanamlilia mchana
na usiku? Je, yeye hatakuwa mvumilivu kwao? 8 Nawaambia kwamba ataleta
haki kwao upesi. Lakini wakati Mwana wa Adamu atakapokuja, je, atakuta imani
duniani? ' 9 Ndipo akawaambia mfano huu kwa baadhi ya watu ambao wanajiona
wenyewe kuwa wenye haki na kuwadharau watu wengine, 10 'Watu wawili walipanda
kwenda hekaluni kusali: mmoja Mfarisayo mwingine mtoza ushuru. 11 Farisayo
akasimama akaomba mambo haya juu yake mwenyewe, 'Mungu, nakushukuru kwa
vile mimi si kama watu wengine ambao ni wanyang'anyi, watu wasio waadilifu,
wazinzi, au kama huyu mtoza ushuru. 12 Nafunga mara mbili kila wiki. Natoa
zaka katika mapato yote ninayopata. ' 13 Lakini yule mtoza ushuru, alisimama
mbali, bila hakuweza hata kuinua macho yake mbinguni, akagonga kifua chake
akisema, 'Mungu, nirehemu mimi mwenye dhambi.' 14 Nawaambia, mtu huyu
alirudi nyumbani akiwa amehesabiwa haki kuliko yule mwingine, kwa sababu kila
ajikwezaye atashushwa, lakini kila mtu anayejinyenyekeza atainuliwa. ' 15 Watu
walimletea watoto wao wachanga, ili aweze kuwagusa, lakini wanafunzi wake
walipoona hayo, wakawazuia. 16 Lakini Yesu akawaita kwake akisema, 'Waacheni
watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie. Maana ufalme wa Mungu ni wa
watu kama hao. 17 Amin, nawaambia, mtu yeyote asiyeupokea ufalme wa Mungu
kama mtoto ni dhahiri hatauingia. ' 18 Mtawala mmoja akamwuliza, akisema,
'Mwalimu mwema, nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?' 19 Yesu akamwambia,
'Kwa nini unaniita mwema? Hakuna mtu aliye mwema, ila Mungu peke yake.
20 Unazijua amri- usizini, usiue, Usiibe, usishuhudie uongo, waheshimu baba yako
na mama yako. 21 Yule mtawala akasema, 'Mambo haya yote nimeyashika tangu
nilipokuwa kijana.' 22 Yesu alipoyasikia hayo akamwambia, '“Umepungukiwa jambo
moja. Lazima uuze vyote ulivyonavyo na uwagawie maskini, nawe utakuwa na
hazina mbinguni -kisha njoo, unifuate. ' 23 Lakini tajiri aliposikia hayo, alihuzunika
sana, kwa sababu alikuwa tajiri sana. 24 Kisha Yesu, akamwona alivyohuzunika sana
akasema, 'Jinsi gani itakavyokuwa vigumu kwa matajiri kuingia katika Ufalme wa
Mungu! 25 Maana ni rahisi sana kwa ngamia kupita katika tundu la sindano, kuliko
kwa tajiri kuingia katika Ufalme wa Mungu. ' 26 Wale waliosikia hayo, wakasema,
'Nani basi, atakayeweza kuokolewa?' 27 Yesu akajibu, 'Mambo yasiyowezekana kwa

mwanadamu kwa Mungu yanawezekana.” 28 Petro akasema, 'Naam, sisi tumeacha
kila kitu na tumekufuata wewe. ' 29 Kisha Yesu akawaambia, Amin, nawaambia
kwamba hakuna mtu aliyeacha nyumba, au mke, au ndugu, au wazazi au watoto,
kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, 30 ambaye hatapokea mengi zaidi katika ulimwengu
huu, na katika ulimwengu ujao, uzima wa milele. ' 31 Baada ya kuwakusanya wale
kumi na wawibili, akawaambia, 'Tazama, tunapanda kwenda Yerusalemu, na mambo
yote ambayo yameandikwa na manabii kuhusu Mwana wa Adamu yatakamilishwa.
32 Kwa maana atatiwa mikononi mwa watu wa Mataifa na atatendewa dhihaka na
jeuri, na kutemewa mate. 33 Baada ya kumchapa viboko watamwua na siku ya
tatu atafufuka. ' 34 Hawakuelewa mambo haya, na neno hili lilikuwa limefichwa
kwao, na hawakuelewa mambo yaliyosemwa. 35 Ikawa Yesu ulipokaribia Yeriko, mtu
mmoja kipofu alikuwa ameketi kando ya barabara akiomba msaada, 36 aliposikia
umati wa watu ukipita aliuliza nini kinatokea. 37 Wakamwambia kwamba Yesu wa
Nazareti anapita. 38 Hivyo yule kipofu akalia kwa sauti, akisema, 'Yesu, Mwana
wa Daudi, unirehemu.' 39 wale waliokuwa wakitembea walimkemea huyo kipofu,
wakamwambia anyamaze. Lakini yeye akazidi kulia kwa sauti, 'Mwana wa Daudi,
unirehemu. 40 Yesu akasimama akaamuru mtu yule aletwe kwake. Kisha yule kipofu
alipomkaribia, Yesu akamwuliza, 41 'Unataka nikufanyie nini?' Akasema, 'Bwana,
nataka kuona.' 42 Yesu akamwambia, 'Upate kuona. Imani yako imekuponya. '
43 Mara hiyo akapata kuona, akamfuata Yesu akimtukuza Mungu. Walipoona hili,
watu wote wakamsifu Mungu.

# 19

1 Yesu aliingia na kupita katikati ya Yeriko. 2 Na hapo palikuwa na mtu mmoja
aitwaye Zakayo. Ambaye alikuwa mkuu wa watoza ushuru tena mtu tajiri. 3 Alikuwa
anajaribu kumwona Yesu ni mtu wa namna gani, lakini hakuweza kuona kwa
sababu ya umati wa watu, kwa kuwa alikuwa mfupi wa kimo. 4 Hivyo, alitangulia
mbio mbele za watu, akapanda juu ya mkuyu ili aweze kumwona, kwa sababu
Yesu alikaribia kupita njia hiyo. 5 Wakati Yesu alipofika mahali pale, aliangalia
juu akamwambia, 'Zakayo, shuka upesi, maana leo ni lazima nishinde nyumbani
mwako.' 6 Akafanya haraka, akashuka na kumkaribisha kwa furaha. 7 Watu wote
walipoona hayo, wakalalamika, wakisema, 'Amekwenda kumtembelea mtu mwenye
dhambi.' 8 Zakayo akasimama akamwambia Bwana, Tazama Bwana nusu ya mali
yangu nawapa maskini, na ikiwa nimemnyang'anya mtu yeyote kitu, nitamrudishia
mara nne. ' 9 Yesu akamwambia, 'Leo wokovu umefika katika nyumba hii, kwa
sababu yeye pia ni mwana wa Ibrahimu. 10 Kwa maana Mwana wa Mtu amekuja
kutafuta na kuokoa watu waliopotea. ' 11 Waliposikia hayo, aliendelea kuongea
na alitoa mfano, kwa sababu alikuwa karibu na Yerusalemu, na wao walidhani
ya kuwa ufalme wa Mungu ulikuwa karibu kuonekana mara moja. 12 Hivyo
akawaambia, 'Ofisa mmoja alikwenda nchi ya mbali ili apokee ufalme na kisha
aurudi. 13 Aliwaita watumishi wake kumi, akawapa mafungu kumi, akawaambia,
'fanyeni biashara mpaka nitakaporudi.' 14 Lakini wananchi wake walimchukia
na hivyo wakatuma wajumbe waende kumfuata na kusema, 'Hatutaki mtu huyu
atutawale.' 15 Ikawa aliporudi nyumbani baada ya kufanywa mfalme, akaamuru
wale watumishi aliokuwa amewaachia fedha waitwe kwake, apate kujua faida gani
waliyoipata kwa kufanya biashara. 16 Wa kwanza akaja, akasema, `Bwana, fungu
lako limefanya mafungu kumi zaidi. ' 17 Huyo Ofisa akamwambia, Vema, mtumishi
mwema. Kwa sababu ulikuwa mwaminifu katika jambo dogo, utakuwa na madaraka
juu ya miji kumi. ' 18 Wa pili akaja, akasema, 'Bwana, fungu lako limefanya mafungu
matano.' 19 Huyo Afisa akamwambia, 'Chukua mamlaka juu ya miji mitano.' 20 Na

mwingine akaja, akasema, `Bwana hii hapa fedha yako, ambayo niliihifadhi salama
katika kitambaa, 21 kwa maana niliogopa kwa sababu wewe ni mtu mkali. Unaondoa
kile usichokiweka na kuvuna usichopanda. ' 22 Huyo Ofisa akamwambia, 'Kwa
maneno yako mwenyewe, nitakuhukumu, ewe mtumishi mbaya. Ulijua kwamba
mimi ni mtu mkali, nachukua nisichokiweka na kuvuna ambacho sikupanda. 23 Basi,
mbona hukuweka fedha yangu katika benki, ili nikirudi niichukue pamoja na
faida? 24 Ofisa akawaambia watu waliokuwa wamesimama hapo, 'Mnyang'anyeni
hilo fungu na kumpa yule mwenye mafungu kumi.' 25 Wakamwambia, `Bwana,
yeye ana mafungu kumi. ' 26 'Nawaambia, kila mtu ambaye anacho atapewa
zaidi, lakini ambaye hana, hata kile alicho nacho kitachukuliwa. 27 Lakini hawa
maadui zangu, ambao hawakutaka niwe Mfalme wao, waleteni hapa na kuwaua
mbele yangu. '' 28 Baada ya kusema hayo, aliendelea mbele akipanda kwenda
Yerusalemu. 29 Ikawa alipokaribia Bethfage na Bethania, karibu na mlima wa
Mizeituni, aliwatuma wanafunzi wake wawili, 30 akisema: `Nendeni katika kijiji cha
jirani. Mkiingia, mtakuta mwana-punda hajapandwa bado. Mfungueni, mkamlete
kwangu. 31 Kama mtu akiwauliza, `Mbona mnamfungua? ' Semeni, “Bwana
anamhitaji. '' 32 Wale waliotumwa wakaenda wakamwona mwana-punda kama Yesu
alivyokuwa amewaambia. 33 Walipokuwa wanamfungua mwana punda wamiliki
wakawaambia, 'Kwa nini mnamfungua mwana punda huyu?' 34 Wakasema, `Bwana
anamhitaji. ' 35 Basi, wakampelekea Yesu, wakatandika nguo zao juu ya mwana
punda na wakampandisha Yesu juu yake. 36 Alipokuwa akienda watu wakatandaza
mavazi yao barabarani. 37 Alipokuwa anateremka mlima wa Mizeituni, jumuiya
yote ya wanafunzi wakaanza kushangilia na kumtukuza Mungu kwa sauti kubwa,
kwa sababu ya mambo makuu waliyoyaona, 38 wakisema, 'Ndiye mbarikiwa Mfalme
ajaye kwa jina la Bwana! Amani mbinguni, na utukufu juu!' 39 Baadhi ya Mafarisayo
katika mkutano wakamwambia, Mwalimu, wanyamazishe wanafunzi wako. ' 40 Yesu
akajibu, akasema, `Nawaambieni, kama hawa wakinyamaza, mawe yatapaza sauti.
' 41 Yesu alipoukaribia mji aliulilia, 42 akisema, laiti ungelijua hata wewe, katika
siku hii mambo ambayo yanayokuletea amani! Lakini sasa yamefichika machoni
pako. 43 Kwa kuwa siku zinakuja ambapo adui zako watajenga boma karibu na
wewe, na kukuzunguka na kukukandamiza kutoka kila upande. 44 Watakuangusha
chini wewe na watoto wako. Hawatakuachia hata jiwe moja juu ya jingine,
kwa sababu haukutambua wakati Mungu alipokuwa anajaribu kukuokoa'. 45 Yesu
aliingia Hekaluni, akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza, 46 akiwaambia,
“Imeandikwa, 'Nyumba yangu itakuwa nyumba ya sala,' lakini ninyi mmeifanya
kuwa pango la wanyang'anyi”. 47 Kwa hiyo, Yesu alikuwa akifundisha kila siku
hekaluni. Makuhani wakuu na walimu wa Sheria na viongozi wa watu walitaka
kumuua, 48 lakini hawakuweza kupata njia ya kufanya hivyo, kwa sababu watu wote
walikuwa wakimsikiliza kwa makini.

# 20

1 Ikawa siku moja, Yesu alipokuwa akiwafundisha watu Hekaluni na kuhubiri
injili, makuhani wakuu na walimu wa Sheria walimwendea pamoja na wazee.
2 Walizungumza, wakimwambia, 'Tuambie ni kwa mamlaka gani unafanya mambo
haya? Au ni nani huyo ambaye amekupa mamlaka haya? “ 3 Naye akajibu,
akawaambia, 'Nami pia nitawauliza swali. Niambieni 4 ubatizo wa Yohana. Je,
ulitoka mbinguni ama kwa watu? ' 5 Lakini wakajadiliana wao kwa wao, wakisema,
'Tukisema, `litoka mbinguni, atatuuliza, ` Basi, mbona hamkumwamini?' 6 Na
tukisema; ilitoka kwa wanadamu; watu wote hapa watatupiga mawe, maana wote
wanaamini kwamba Yohana alikuwa nabii. ' 7 Basi, wakamjibu ya kwamba

hawakujua ilikotoka. 8 Yesu akawaambia, '“Wala mimi siwaambii ninyi ni kwa
mamlaka gani ninafanya mambo haya.” 9 Aliwaambia watu mfano huu, “Mtu
mmoja alipanda shamba la mizabibu, akalikodisha kwa wakulima wa mizabibu,
na akaenda nchi nyingine kwa muda mrefu. 10 Kwa muda uliopangwa, alimtuma
mtumishi kwa wakulima mizabibu, kwamba wampe sehemu ya matunda ya shamba
la mizabibu. Lakini wakulima wa mzabibu wakampiga, wakamrudisha mikono-
mitupu. 11 Kisha akamtuma tena mtumishi mwingine na nao wakampiga, kumtendea
vibaya, na wakamrudisha mikono- mitupu. 12 Alimtuma tena wa tatu na nao
wakamjeruhi na kumtupa nje. 13 Hivyo bwana wa shamba akasema, 'Nitafanya
nini? Nitamtuma mwanangu mpendwa. Labda watamheshimu. ' 14 Lakini
wakulima wa mzabibu walipomwona, walijadili wao kwa wao wakisema, `Huyu
ndiye mrithi. Tumuue, ili urithi wake uwe wetu. ' 15 Wakamtoa nje ya shamba la
mizabibu na kumuua. Je bwana shamba atawafanya nini? 16 Atakuja kuwaangamiza
wakulima wa mzabibu, na atawapa shamba hilo wengine”. 'Nao waliposikia hayo,
wakasema, 'Mungu amekataa' 17 Lakini Yesu akawatazama, akasema, “Je andiko
hili lina maana gani? 'Jiwe walilolikataa wajenzi, limekuwa jiwe la pembeni'?
18 Kila mtu aangukaye juu ya jiwe hilo, atavunjika vipande vipande. Lakini yule
ambaye litamwangukia, litamponda. ' 19 Hivyo waandishi na wakuu wa makuhani
walitafuta njia ya kumkamata wakati huohuo, walijua kwamba alikuwa amesema
mfano huu dhidi yao. Lakini waliwaogopa watu. 20 Walimuangalia kwa makini,
wakatuma wapelelezi waliojifanya kuwa watu wa haki, ili wapate kupata kosa kwa
hotuba yake, ili kumpelekakwa watawala na wenye mamlaka. 21 Nao wakamwuliza,
wakisema, “Mwalimu, tunajua kwamba unasema na kufundisha mambo ya kweli
na si kushawishiwa na mtu yeyote, lakini wewe hufundisha ukweli kuhusu njia
ya Mungu. 22 Je, ni halali kwetu kulipa kodi kwa Kaisari, au la?” 23 Lakini Yesu
alitambua mtego wao, akawaambia, 24 “Nionyesheni dinari. Sura na chapa ya
nani ipo juu yake?” Walisema, '“Ya Kaisari.” 25 Naye akawaambia, 'Basi, mpeni
Kaisari yaliyo yake Kaisari, na Mungu yaliyo yake Mungu.' 26 Waandishi na wakuu
wa makuhani hawakuwa na uwezo wa kukosoa kile alichosema mbele ya watu.
Wakastaajabia majibu yake na hawakusema chochote. 27 Baadhi ya Masadukayo
wakamwendea, wale ambao wanasema kwamba hakuna ufufuo, 28 wakamwuliza,
wakisema, “Mwalimu, Musa alituandikia kwamba kama mtu akifiwa na ndugu
mwenye mke ambaye hana mtoto basi anapaswa kumchukuna mke wa ndugu yake
na kuzaa nae kwa ajili ya kaka yake. 29 Kulikuwa na ndugu saba Wa kwanza alioa,
akafa bila kuacha mtoto, 30 na wa pili pia. 31 Wa tatu akamchukua vilevile, vivyo
hivyo wa saba hakuacha watoto na akafa. 32 Baadaye yule mwanamke pia akafa.
33 Katika ufufuo atakuwa mke wa nani? Maana wote saba walikuwa wamemwoa. '
34 Yesu akawaambia, “Wana wa ulimwengu huu huoa na kuolewa. 35 Lakini wale
wanastaohili kupokea ufufuo wa wafu na kuingia uzima wa milele hawaoi wala
hawaolewi. 36 Wala hawawezi kufa tena, kwa sababu huwa sawasawa na malaika
na ni watoto wa Mungu, wana wa ufufuo. 37 Lakini hiyo wafu wanafufuliwa, hata
Musa alionyesha mahali katika habari za kichaka, pale alimwita Bwana kama Mungu
wa Ibrahimu na Mungu wa Isaka na Mungu wa Yakobo. 38 Sasa, yeye si Mungu wa
wafu, bali wa walio hai, kwa sababu wote huishi kwake. “ 39 Baadhi ya walimu
wa Sheria wakamjibu, 'Mwalimu, umejibu vema. ' 40 Hawakuthubutu kumwuliza
maswali mengine zaidi. 41 Yesu akawaambia, “Ki vipi watu wanasema kwamba
Kristo ni mwana wa Daudi? 42 Maana Daudi mwenyewe anasema katika Zaburi:
Bwana alimwambia Bwana wangu: Keti mkono wa kulia, 43 mpaka niwaweke adui
zako chini ya miguu yako. ' 44 Daudi anamwita Kristo 'Bwana', basi atakuwaje
mwana wa Daudi?” 45 Watu wote walipokuwa wakimsikiliza akawaambia wanafunzi

wake, 46 'Jihadharini na waandishi, wapendao kutembea wamevaa mavazi marefu, na
wapenda salamu maalum sokoni na viti vya heshima katika masinagogi, na maeneo
ya heshima karamuni. 47 Wao pia hula nyumba za wajane, na wanajifanya wanasali
sala ndefu. Hawa watapokea hukumu kubwa zaidi. '

# 21

1 Yesu alitazama akawaona wanaume matajiri waliokuwa wanaweka zawadi zao
kwenye hazina. 2 Akamuona mjane mmoja masikini akiweka senti zake mbili.
3 Hivyo akasema, “Kweli nawaambieni, huyu Mjane maskini ameweka nyingi kuliko
wengine wote. 4 Hawa wote wametoa hizi zawadi kutoka katika vingi walivyonavyo.
Lakini huyu mjane, katika umaskini wake, ametoa fedha zote alizokuwa nazo
kwa ajili ya kuishi kwake.” 5 Wakati wengine walipokuwa wakisema juu ya
hekalu, namna lilivyokuwa limepambwa na mawe mazuri na matoleo, alisema,
6 “Kwa habari ya mambo haya mnayoyaona, siku zitakuja ambazo hakuna jiwe
moja ambalo litaachwa juu ya jiwe jingine ambalo halitabomolewa.” 7 Hivyo
wakamuuliza, wakasema, “Mwalimu, mambo haya yatatokea lini? Na nini ni
itakuwa ishara kwamba haya mambo yako karibu kutokea?” 8 Yesu akajibu, “Muwe
waangalifu kwamba msidanganywe. Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu,
wakisema, 'Mimi ndiye, 'na 'Muda umekaribia'. Msiwafuate. 9 Mkisikia vita na
vuruguvurugu msiogope, kwa sababu haya mambo lazima yatokee kwanza, lakini
mwisho hautatokea upesi.” 10 Kisha akawaambia, “Taifa litainuka kupigana na taifa
jingine, na ufalme juu ya ufalme mwingine. 11 Kutakuwa na matetemeko makubwa,
na njaa na tauni katika maeneo mbalimbali. Kutakuwa na matukio ya kutisha na
ishara za kutisha kutoka mbinguni. 12 Lakini kabla ya mambo haya yote, wataweka
mikono yao juu yenu na kuwatesa, kuwapeleka kwenye masinagogi na magereza,
kuwaleta mbele za wafalme na wenye mamlaka kwa sababu ya jina langu. 13 Hii
itawafungulia fursa kwa ushuhuda wenu. 14 Kwahiyo amueni mioyoni mwenu
kutoandaa utetezi wenu mapema, 15 kwa sababu nitawapa maneno na hekima,
ambayo adui zenu wote hawataweza kuipinga au kuikana. 16 Lakini mtakataliwa
pia na wazazi wenu, ndugu zenu, jamaa zenu na rafiki zenu, na watawaua baadhi
yenu. 17 Mtachukiwa na kila mmoja kwa sababu ya jina langu. 18 Lakini hakuna
hata unywele mmoja wa vichwa vyenu utakaopotea. 19 Katika kuvumilia mtaziponya
nafsi zenu. 20 Mtakapoona Yerusalemu imezungukwa na majeshi, basi jueni kwamba
uharibifu wake umekaribia. 21 Hapo wale walioko Yudea wakimbilie milimani,
na wale walioko katikati ya jiji waondoke, na msiwaache walioko vijijini kuingia.
22 Maana hizi ni siku za kisasi, ili kwamba mambo yote yaliyoandikwa yapate
kutimilika. 23 Ole ni kwa wale walio na mimba na kwa wale wanyonyeshao katika
siku hizo! Kwa maana kutakuwa na adha kuu juu ya nchi, na ghadhabu kwa
watu hawa. 24 Na wataanguka kwa ncha ya upanga na watachukuliwa mateka
kwa mataifa yote, na Yerusalem itakanyagwa na watu wa mataifa, mpaka wakati
wa watu wa mataifa utakapotimilika. 25 Kutakuwa na ishara katika jua, mwezi
na nyota. Na katika nchi kutakuwa na dhiki ya mataifa, katika kukata tamaa
kutokana na mlio wa bahari na mawimbi. 26 Kutakuwa na watu wakizimia kwa
hofu na katika kutarajia mambo yatakoyo tokea juu ya dunia. Kwa maana nguvu za
mbingu zitatikiswa. 27 Kisha watamwona Mwana wa Adamu akija mawinguni katika
nguvu na utukufu mkuu. 28 Lakini mambo haya yatakapoanza kutokea, simameni,
inueni vichwa vyenu, kwa sababu ukombozi wenu umesogea karibu.” 29 Yesu
akawaambia kwa mfano, “Uangalieni mtini, na miti yote. 30 Inapotoa machipukizi,
mnajionea wenyewe na kutambua kwamba kiangazi tayari kiko karibu. 31 Vivyo
hivyo, mnapoona mambo haya yanatokea, ninyi tambueni ya kwamba ufalme wa

Mungu umekaribia. 32 Kweli, nawaambieni, kizazi hiki hakitapita, mpaka mambo
haya yote yatakapotokea. 33 Mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yangu hayatapita
kamwe. 34 Lakini jiangalieni wenyewe, ili kwamba mioyo yenu isije ikalemewa na
ufisadi, ulevi, na mahangaiko ya maisha haya. Kwa sababu ile siku itawajia ghafla
35 kama mtego. Kwasababu itakuwa juu ya kila mmoja aishiye katika uso wa dunia
nzima. 36 Lakini mwe tayari wakati wote, mwombe kwamba mtakuwa imara vya
kutosha kuyaepuka haya yote yatakayotokea, na kusimama mbele za Mwana wa
Adamu." 37 Hivyo wakati wa mchana alikuwa akifundisha hekaluni na usiku alitoka
nje, na kwenda kukesha katika mlima unaoitwa wa Mzeituni. 38 Watu wote walimjia
asubuhi na mapemaili kumsikiliza ndani ya hekalu.

# 22

1 Basi Sikukuu ya Mkate Usiyotiwa Chachu ilikuwa imekaribia, ambayo inaitwa
Pasaka. 2 Makuhani wakuu na waandishi wakajadiliana namna ya kumuua Yesu,
kwa sababu waliwaogopa watu. 3 Shetani akaingia ndani ya Yuda Iskariote, mmoja
wa wale wanafunzi Kumi na mbili. 4 Yuda akaenda kujadiliana na wakuu wa
makuhani na wakuu namna ambavyo atamkabidhi Yesu kwao. 5 Walifurahi, na
kukubaliana kumpa fedha. 6 Yeye aliridhia, na alitafuta fursa ya kumkabidhi Yesu
kwao mbali na kundi la watu. 7 Siku ya mikate isiyotiwa chachu ikafika, ambapo
kondoo wa Pasaka lazima atolewe. 8 Yesu akawatuma Petro na Yohana, akasema,
"Nendeni mkatuandalie chakula cha Pasaka ili tuje tukile." 9 Wakamuuliza, "Wapi
unataka tuyafanyie hayo maandalizi?" 10 Akawajibu, "Sikilizeni, mtakapokuwa
mmeingia mjini, mwanamume ambaye amebeba mtungi wa maji atakutana na
ninyi. Mfuateni kwenye nyumba ambayo ataingia. 11 Kisha mwambieni bwana
wa nyumba, "Mwalimu anakwambia, "Kiko wapi chumba cha wageni, mahali
ambapo nitakula Pasaka na wanafunzi wangu?" 12 Atawaonyesha chumba cha
ghorofani ambacho kiko tayari. Fanyeni maandalizi humo." 13 Hivyo wakaenda,
na wakakuta kila kitu kama alivyowaambia. Kisha wakaandaa chakula cha Pasaka.
14 Muda ulipofika alikaa na wale mitume. 15 Kisha akawaambia, "Nina shauku
kubwa ya kula sikukuu hii ya Pasaka na ninyi kabla ya kuteswa kwangu. 16 Kwa
maana nawaambieni, sitakula tena mpaka itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu."
17 Kisha Yesu akachukua kikombe, na alipokwisha kushukuru, akasema, "Chukueni
hiki, na mgawane ninyi kwa ninyi. 18 Kwa maana nawaambia, sitakunywa tena
mzao wa mzabibu, mpaka ufalme wa Mungu utakapokuja." 19 Kisha akachukua
mkate, na alipokwisha kushukuru, akaumega, na kuwapa, akisema, "Huu ni mwili
wangu ambao umetolewa kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa kunikumbuka mimi."
20 Akachukua kikombe vivyo hivyo baada ya chakula cha usiku akisema, "Kikombe
hiki ni agano jipya katika damu yangu, ambayo imemwagika kwa ajili yenu. 21 Lakini
angalieni. Yule anisalitie yuko pamoja nami mezani. 22 Kwa maana Mwana wa
Adamu kwa kweli aenda zake kama ilivyokwisha amuliwa. Lakini ole kwa mtu
yule ambaye kupitia yeye Mwana wa Adamu asalitiwa!" 23 Wakaanza kuulizana wao
kwa wao, nani miongoni mwao ambaye angefanya jambo hili. 24 Kisha yakatokea
mabishano katikati yao kwamba ni nani anaye dhaniwa kuwa mkuu kuliko wote.
25 Akawaambia, "Wafalme wa watu wa mataifa wana ubwana juu yao, na wale
mwenye mamlaka juu yao wanaitwa waheshimiwa watawala. 26 Lakini haitakiwi
kabisa kuwa hivi kwenu ninyi. Badala yake, acha yule ambaye ni mkubwa kati
yenu awe kama mdogo. Na yule ambaye ni wa muhimu sana awe kama atumikaye.
27 Kwa sababu yupi mkubwa, yule akaaye mezani au yule anayetumika? Je si yule
aketie mezani? Na mimi bado ni kati yenu kama atumikaye. 28 Lakini ninyi ndio
ambao mmeendelea kuwa nami katika majaribu yangu. 29 Nawapa ninyi ufalme,

kama vile Baba alivyonipa mimi ufalme, 30 kwamba mpate kula na kunywa mezani
kwangu kwenye ufalme wangu. Na mtakaa kwenye viti vya enzi mkizihukumu kabila
kumi na mbili za Israel. 31 Simoni, Simoni, fahamu kwamba, Shetani ameomba
awapate ili awapepete kama ngano. 32 Lakini nimekuombea, kwamba imani yako
isishindwe. Baada ya kuwa umerudi tena, waimarishe ndugu zako.” 33 Petro
akamwambia, “Bwana, niko tayari kwenda na wewe gerezani na hata katika mauti.”
34 Yesu akajibu, “Nakwambia, Petro, Jogoo hatawika leo, kabla hujanikana mara tatu
kwamba unanijua.” 35 Kisha Yesu akawaambia, “Nilipowapeleka ninyi bila mfuko,
kikapu cha vyakula, ua viatu, je mlipungukiwa na kitu?” Wakajibu “Hakuna.”
36 Kisha akawaambia, “Lakini sasa, kila mwenye mfuko, na auchukue pamoja na
kikapu cha vyakula. Yule ambaye hana upanga imempasa auze joho lake anunue
mmoja. 37 Kwa sababu nawaambia, yote ambayo yameandikwa kwa ajili yangu
lazima yatimilike, 'Na alichukuliwa kama mtu ambaye anavunja torati.' Kwa sababu
kile kilichotabiriwa kwa ajili yangu kinatimizwa.” 38 Kisha wakasema, “Bwana,
tazama! Hizi hapa panga mbili.” Na akawaambia”yatosha.” 39 Baada ya chakula cha
usiku, Yesu aliondoka, kama ambavyo amekuwa akifanya mara kwa mara, akaenda
mlima wa Mzeituni, na wanafunzi wakamfuata. 40 Walipofika, aliwaambia, “Ombeni
kwamba msiingie majaribuni.” 41 Akaenda mbali na wao kama mrusho wa jiwe,
akapiga magoti akaomba, 42 akisema, “Baba, kama unataka, niondolee kikombe
hiki. Lakini si kama nitakavyo mimi, lakini mapenzi yako yafanyike.” 43 Kisha
malaika kutoka mbinguni akamtokea, akamtia nguvu. 44 Akiwa katika kuugua,
akaomba kwa dhati zaidi, na jasho lake likawa kama matone makubwa ya damu
yakidondoka chini. 45 Wakati alipoamka kutoka katika maombi yake, alikuja kwa
wanafunzi, na akawakuta wamelala kwa sababu ya huzuni yao, 46 na akawauliza,
“Kwanini mnalala? Amkeni muombe, kwamba msiingie majaribuni.” 47 Wakati
alipokuwa bado akiongea, tazama, kundi kubwa la watu likatokea, na Yuda, mmoja
wa mitume kumi na wawili akiwaongoza. Akaja karibu na Yesu ili ambusu, 48 lakini
Yesu akamwambia, “Yuda, je unamsaliti Mwana wa Adamu kwa busu?” 49 Wakati
wale waliokuwa karibu na Yesu walipoona hayo yanayotokea, wakasema, “Bwana,
je tuwapige kwa upanga?” 50 Kisha mmoja wao akampiga mtumishi wa kuhani
mkuu, akamkata sikio lake la kulia. 51 Yesu akasema, “hii inatosha. Na akagusa
sikio lake, akamponya. 52 Yesu akasema kwa kuhani mkuu, na kwa wakuu wa
hekalu, na kwa wazee waliokuja kinyume chake, “Je mnakuja kana kwamba mnakuja
kupambana na mnyang'anyi, na marungu na mapanga? 53 Nilipokuwa pamoja nanyi
siku zote kwenye hekalu, hamkuweka mikono yenu juu yangu. Lakini hii ni saa
yako, na mamlaka ya giza.” 54 Wakamkamata, wakamuongoza, wakamleta nyumbani
mwa kuhani mkuu. Lakini Petro akamfuatilia kwa mbali. 55 Baada ya kuwa
wamewasha moto katika ule uwanda wa ndani na walipokwisha kukaa chini pamoja,
Petro akakaa katikati yao. 56 Mtumishi mmoja wa kike akamuona Petro alipokuwa
amekaa katika mwanga utokanao na moto, akamtazama akamwambia, “Huyu mtu
pia alikuwa pamoja naye.” 57 Lakini Petro akakana, akasema, “mwanamke, mimi
simjui.” 58 Baada ya muda kidogo, mtu mwingine akamuona akasema “Wewe pia
ni mmoja wao”. Lakini Petro akajibu, “Mwanaume, mimi siyo.” 59 Baada ya kama
saa moja hivi, mwanaume mmoja akasisitiza akasema, “Kweli kabisa huyu mtu pia
alikuwa pamoja naye, maana ni Mgalilaya.” 60 Lakini Petro akasema, “Mwanaume,
sijui usemalo.” Na mara, wakati akiongea, jogoo akawika. 61 Akageuka, Bwana
akamtazama Petro. Na Petro akalikumbuka neno la Bwana, pale alipomwambia,
“Kabla ya jogoo kuwika leo, utanikana mimi mara tatu.” 62 Akienda nje, Petro
akalia kwa uchungu mwingi. 63 Kisha wale wanaume waliokuwa wakimlinda
Yesu, wakamdhihaki na kumpiga. 64 Baada ya kumfunika macho, wakamuuliza,

wakisema, “Tabiri! Ni nani aliyekupiga?” [65] Wakaongea mambo mengine mengi
kinyume cha Yesu na kumkufuru yeye. [66] Mara ilipokuwa asubuhi, wazee wa watu
walikusanyika pamoja, wakuu wa makuhani na waandishi. Wakampeleka kwenye
Baraza, [67] wakisema, “Kama wewe ni Kristo, tuambie.” Lakini yeye akawaambia,
“Kama nikiwaambia, hamtaniamini, [68] na kama nikiwauliza hamtanijibu.” [69] Lakini
kuanzia sasa na kuendelea, Mwana wa Adamu atakuwa amekaa mkono wa kuume
wa nguvu ya Mungu.” [70] Wote wakasema, “Kwa hiyo wewe ni Mwana wa Mungu?”
Na Yesu akawaambia, “Ninyi mmesema mimi ndiye.” [71] Wakasema, “Kwa nini bado
tunahitaji tena ushahidi? Kwa sababu sisi wenyewe tumesikia kutoka katika kinywa
chake mwenyewe.”

# 23

[1] Mkutano wote wakasimama, wakampeleka Yesu mbele ya Pilato. [2] Wakaanza
kumshutumu, wakisema, “Tumemkuta mtu huyu akipotosha taifa letu, kwa kukataza
tusitoe kodi kwa Kaisari, na akisema kwamba yeye mwenyewe ni Kristo, Mfalme.”
[3] Pilato akamuuliza, akisema, “Je wewe ni Mfalme wa Wayahudi?” Na Yesu akamjibu
akisema, “Wewe wasema hivyo”. [4] Pilato akamuambia kuhani mkuu na makutano,
“Sioni kosa kwa mtu huyu”. [5] Lakini wao wakasisitiza, wakisema, “ Amekuwa
akiwachochea watu, akifundisha katika Uyahudi yote, kuanzia Galilaya na sasa
yuko hapa.” [6] Pilato aliposikia haya, akaulizia kama mtu huyo ni wa Galilaya?
[7] Alipotambua kuwa alikuwa chini ya utawala wa Herode, akampeleka Yesu kwa
Herode, ambaye naye alikuwa Yerusalemu kwa siku hizo. [8] Herode alipomuona
Yesu, alifurahi sana kwasababu alitaka kumuona kwa siku nyingi. Alisikia habari
zake na alitamani kuona moja ya miujiza ikifanywa na yeye. [9] Herode alimhoji
Yesu kwa maneno mengi, lakini Yesu hakumjibu chochote. [10] Makuhani wakuu
pamoja na waandishi walisimama kwa ukali wakimshitaki. [11] Herode pamoja na
maaskari wake, walimtukana na kumdhihaki, na kumvika mavazi mazuri, kisha
akamrudisha Yesu kwa Pilato. [12] Herode na Pilato wakawa marafiki kuanzia siku
hiyo, (kabla ya hapo walikuwa maadui). [13] Pilato akawaita pomoja makuhani wakuu
na watawala na umati wa watu, [14] Akawaambia, “Mmeniletea mtu huyu kama mtu
anaye waongoza watu wafanye mabaya, na tazama, baada ya kuwa nimemhoji mbele
yenu, sikuona kosa kwa mtu huyu kuhusu mambo yote ambayo ninyi mnamshitaki
yeye. [15] Hapana, wala Herode, kwa maana amemrudisha kwetu, na tazama
hakuna chochote alichokifanya kinachostahili adhabu ya kifo. [16] Kwahiyo basi
nitamuadhibu na kumuachilia. [17] (Sasa, Pilato anawajibika kumuachilia mfungwa
mmoja kwa wayahudi wakati wa sikukuu). [18] Lakini wote wakapiga kelele pamoja,
wakisema, “Mwondoe huyo, na tufungulie Baraba!” [19] Baraba alikuwa ni mtu
ambaye amewekwa gerezani kwa sababu ya uasi fulani katika jiji na kwa kuua.
[20] Pilato akawaambia tena, akitamani kumwachilia Yesu. [21] Lakini wao wakapiga
kelele, wakisema, “Msulibishe, msulibishe.” [22] Akawauliza kwa mara ya tatu, “kwa
nini, huyu mtu amefanya maovu gani? Sikupata kosa linalostahili adhabu ya kifo
kwake. Kwahiyo nitakapo maliza kumuadhibu nitamuachilia.” [23] Lakini wakasisitiza
kwa sauti ya juu, wakitaka asulubiwe. Na sauti zao zikamshawishi Pilato. [24] Hivyo
Pilato akaamua kuwapatia matakwa yao. [25] Akamuachilia yule waliyemtaka ambaye
alifungwa kwa kusababisha ghasia na kuua. Lakini akamtoa Yesu kwa matakwa yao.
[26] Walipokuwa wakimpeleka, walimkamata mtu mmoja aitwaye Simoni wa Ukirene,
akitokea katika nchi, wakamtwika msalaba ili abebe, akimfuata Yesu. [27] umati
mkubwa wa watu, na wanawake ambao walihuzunika na kuomboleza kwa ajili
yake, walikuwa wakimfuata. [28] Lakini akawageukia, Yesu akawaambia, 'Mabinti wa
Yerusalemu, msinililie mimi, bali jililieni ninyi wenyewe na kwa ya ajili watoto wenu.

[29] Tazama, siku zinakuja ambazo watasema, “Wamebarikiwa walio tasa na matumbo
yasiyozaa, na matiti ambayo hayakunyonyesha. [30] Ndipo watakapo anza kuiambia
milima, 'Tuangukieni,' na vilima, 'Mtufunike.' [31] Maana kama wakifanya mambo
haya ikiwa mti mbichi, itakuwaje ukiwa mkavu?” [32] wanaume wengine, wahalifu
wawili, walipelekwa pamoja naye ili wauwawe. [33] Walipofika mahali paitwapo Fuvu
la kichwa, ndipo wakamsulubisha pamoja na wale wahalifu, mmoja upande wa kulia
na mwingine upande wa kushoto. [34] Yesu alisema, “Baba, uwasamehe, kwa kuwa
hawajui watendalo. “Nao wakapiga kura, kugawa mavazi yake. [35] Watu walikuwa
wamesimama wakiangalia huku watawala wakimdhihaki, wakisema, “Aliwaokoa
wengine. Sasa ajiokoe mwenyewe, kama yeye ni Kristo wa Mungu, mteule”.
[36] Askari pia walimdharau, walimkaribia yeye na wakumpa siki, [37] wakisema, “Kama
wewe ni Mfalme wa Wayahudi jiokoe mwenyewe” [38] Kulikuwa pia na alama juu
yake iliyoandikwa “HUYU NDIYE MFALME WA WAYAHUDI.” [39] Mmoja wa wahalifu
aliyesulubishwa alimtukana akisema, “Wewe si Kristo? jiokoe mwenyewe na sisi”
[40] Lakini yule mwingine akajibu, akimkemea na akisema, “Je wewe humuogopi
Mungu, nawe uko katika hukumu hiyo hiyo? [41] Sisi tupo hapa kwa haki, kwa maana
sisi tunapokea kile tunachostahili kwa matendo yetu. Lakini mtu huyu hakufanya
chochote kibaya.” [42] Na aliongeza, “Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme
wako.” [43] Yesu akamwambia, “Amini nakuambia, leo hii utakuwa pamoja nami
Paradiso.” [44] Hapo ilikuwa karibu saa ya sita, giza likaja juu ya nchi yote hadi
saa ya tisa, [45] Mwanga wa jua ulizimika. Kisha pazia la hekalu likagawanyika
katikati kuanzia juu. [46] Akilia kwa sauti kuu, Yesu alisema, “Baba mikononi mwako
naiweka roho yangu,” baada ya kusema haya, akafa. [47] Wakati Akida alipoona
yaliyotendeka alimtukuza Mungu akisema, “Hakika huyu alikuwa mtu mwenye
haki.” [48] Wakati umati wa watu waliokuja pamoja kushuhudia walipoona mambo
yaliyofanyika, walirudi huku wakipiga vifua vyao. [49] Lakini marafiki zake, na
wanawake waliomfuata toka Galilaya, walisimama kwa mbali wakiangalia hayo
mambo. [50] Tazama, palikuwepo na mtu aitwaye Yusufu, ambaye ni mmoja wa baraza,
mtu mzuri na mwenye haki, [51] (alikuwa hajakubaliana na maamuzi au matendo yao),
kutoka Armathaya, mji wa Kiyahudi, ambao ulikua ukisubiria ufalme wa Mungu.
[52] Mtu huyu, alimkaribia Pilato, akaomba apewe mwili wa Yesu. [53] Alimshusha, na
akauzungushia sanda, na akaumweka katika kaburi lililokuwa limechongwa katika
jiwe, ambalo hakuna aliyewahi kuzikwa. [54] Ilikuwa ni siku ya maandalizi, na Sabato
inakaribia. [55] Wanawake, waliokuja nao kutoka Galilaya, walimfuata, na wakaona
kaburi na jinsi mwili wake ulivyolazwa. [56] Walirudi na kuanza kuandaa manukato
na marashi. Kisha siku ya sabato walipumzika kwa mujibu wa sheria.

# 24

[1] Mapema sana siku ya kwanza ya juma, walikuja kaburini, wakileta manukato
ambayo walikuwa wameyaandaa. [2] Wakakuta jiwe limevingirishwa mbali na
kaburi. [3] Wakaingia ndani, lakini hawakuukuta mwili wa Bwana Yesu. [4] Ilitokea
kwamba, wakati wamechanganyikiwa kuhusu hili, ghafla, watu wawili walisimama
katikati yao wamevaa mavazi ya kung'aa. [5] Wanawake wakiwa wamejaa hofu na
wakiinamisha nyuso zao chini, wakawaambia wanawake, “Kwanini mnamtafuta
aliye hai miongoni mwa wafu? [6] Hayupo hapa, ila amefufuka! Kumbukeni
alivyosema nanyi alipokuwa angali Galilaya, [7] akisema kwamba Mwana wa Adamu
lazima atolewe kwenye mikono ya watu wenye dhambi na asulubishwe, na siku ya
tatu, afufuke tena.” [8] Wale wanawake wakakumbuka maneno yake, [9] na wakarudi
kutoka kaburini na wakawaambia mambo haya yote wale kumi na moja na wengine
wote. [10] Basi Maria Magdalena, Joana, Maria mama wa Yakobo, na wanawake

wengine pamoja nao wakatoa taarifa hizi kwa mitume. 11 Lakini ujumbe huu
ukaonekana kama mzaha tu kwa mitume, na hawakuwaamini wale wanawake.
12 Hata hivyo Petro aliamka, na akakimbia kuelekea kaburini, na akichungulia na
kuangalia ndani, aliona sanda peke yake. Petro kisha akaondoka akaenda nyumbani
kwake, akistaajabu nini ambacho kimetokea. 13 Na tazama, wawili miongoni mwao
walikuwa wakienda siku hiyo hiyo katika kijiji kimoja kiitwacho Emmau, ambacho
kilikuwa maili sitini kutoka Yerusalemu. 14 Wakajadiliana wao kwa wao kuhusu
mambo yote yaliyotokea. 15 Ikatokea kwamba, wakati walipokuwa wakijadiliana
na kuulizana maswali, Yesu akasogea karibu akaambatana nao. 16 Lakini macho
yao yalizuiliwa katika kumtambua yeye. 17 Yesu akawaambia, “Nini ambacho ninyi
wawili mnakiongelea wakati mnatembea?” Wakasimama pale wakionekana na
huzuni. 18 Mmoja wao, jina lake Cleopa, akamjibu, “Je wewe ni mtu pekee hapa
Yerusalemu ambaye hajui mambo yaliyotokea huko siku hizi?” 19 Yesu akawaambia,
“Mambo gani?” Wakamjibu, “Mambo kuhusu Yesu Mnazareti, ambaye alikuwa
nabii, muweza katika matendo na maneno mbele za Mungu na watu wote. 20 Na
kwa jinsi ambayo wakuu wa makuhani na viongozi wetu walivyomtoa kuhukumiwa
kifo na kumsulubisha. 21 Lakini tulitumaini kwamba yeye ndiye atakaye waweka
huru Israeli. Ndiyo, mbali na haya yote, sasa ni siku ya tatu tangu mambo haya
yatokee. 22 Lakini pia, baadhi ya wanawake kutoka katika kundi letu walitushangaza,
baada ya kuwapo kaburini asubuhi na mapema. 23 Walipoukosa mwili wake,
wakaja, wakisema kwamba waliona pia maono ya malaika waliosema kwamba
yu hai. 24 Baadhi ya wanaume ambao walikuwa pamoja nasi walienda kaburini,
na kukuta ni kama vile wanawake walivyosema. Lakini hawakumuona yeye.”
25 Yesu akawaambia, “Ninyi watu wajinga na wenye mioyo mizito ya kuamini yote
ambayo manabii wamesema! 26 Je haikuwa lazima Yesu kuteseka kwa mambo
haya, na kuingia katika utukufu wake?” 27 Kisha kuanzia kutoka kwa Musa na
manabii wote, Yesu akawatafsiria mambo yanayomuhusu yeye katika maandiko
yote. 28 Walipokaribia kile kijiji, huko walikokuwa wakienda, Yesu akafanya kana
kwamba anaendelea mbele. 29 Lakini walimlazimisha, wakisema, “Kaa pamoja
nasi, maana inaelekea jioni na siku ni kama imeisha.” Hivyo Yesu akaingia
kwenda kukaa nao. 30 Ilitokea kwamba, wakati amekaa nao kula, alichukua mkate,
akaubariki, na kuuvunja, akawapa. 31 Kisha macho yao yakafunguliwa, wakamjua,
na akatoweka ghafla mbele ya macho yao. 32 Wakasemezana wao kwa wao,
“Hivi mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, wakati alipoongea nasi njiani, wakati
alipotufungulia maandiko?” 33 Wakanyanyuka saa hiyo hiyo, na kurudi Yerusalemu.
Wakawakuta wale kumi na mmoja wamekusanyika pamoja, na wale waliokuwa
pamoja nao, 34 wakisema, “Bwana amefufuka kwelikweli, na amemtokea Simoni.”
35 Hivyo wakawaambia mambo yaliyotokea njiani, na namna Yesu alivyodhihirishwa
kwao katika kuumega mkate. 36 Wakati wakiongea mambo hayo, Yesu mwenyewe
alisimama katikati yao, na akawaambia, “Amani iwe kwenu.” 37 Lakini waliogopa
na kujawa na hofu, na wakafikiri kwamba waliona roho. 38 Yesu akawaambia,
Kwanini mnafadhaika? Kwanini maswali yanainuka mioyoni mwenu? 39 Angalieni
mikono yangu na miguu yangu, kwamba ni mimi mwenyewe. Niguseni na
muone. Kwa maana roho haina nyama na mifupa, kama mnionavyo mimi kuwa
navyo.” 40 Alipokwisha kusema hivi, akawaonyesha mikono yake na miguu yake.
41 Walipokuwa bado na furaha iliyochanganyikana na kutokuamini, na kustaajabu,
Yesu akawaambia, “Je mna kitu chochote cha kula?” 42 Wakampa kipande cha
samaki aliyechomwa. 43 Yesu akakichukua, na kukila mbele yao. 44 Akawaambia,
“Nilipokuwa nanyi, niliwaambia kwamba yote yalioandikwa kwenye sheria ya Musa
na manabii na Zaburi lazima yatimilike.” 45 Kisha akafungua akili zao, kwamba

waweze kuyaelewa maandiko. 46 Akawaambia, “Kwamba imeandikwa, Kristo lazima
ateseke, na kufufuka tena kutoka katika wafu siku ya tatu. 47 Na toba na msamaha
wa dhambi lazima ihubiriwe kwa jina lake kwa mataifa yote, kuanzia kutokea
Yerusalemu. 48 Ninyi ni mashahidi wa mambo haya. 49 Angalia, nawapelekea
ahadi ya Baba yangu juu yenu. Lakini subirini hapa jijini, mpaka mtakapovishwa
nguvu kutoka juu. 50 Kisha Yesu akawaongoza nje mpaka walipokaribia Bethania.
Akainua mikono yake juu, na akawabariki. 51 Ikatokea kwamba, wakati alipokuwa
akiwabariki, aliwaacha na akabebwa juu kuelekea mbinguni. 52 Basi wakamwabudu,
na kurudi Yerusalemu na furaha kuu. 53 Waliendelea kuwepo hekaluni, wakimbariki
Mungu.

# Yohana

[1] Mwanzoni kulikuwako Neno, na Neno alikuwa pamoja na Mungu, na Neno
alikuwa Mungu. [2] Huyu, Neno, Mwanzoni alikuwa pamoja na Mungu. [3] Vitu
vyote vilifanyika kupitia yeye, na pasipo yeye hakuna hata kitu kimoja kilichokuwa
kimefanyika. [4] Ndani yake kulikuwa uzima, na huo uzima ulikuwa nuru ya
wanadamu wote. [5] Nuru yang'aa gizani, wala giza halikuizimisha. [6] Palikuwa na
mtu aliyetumwa kutoka kwa Mungu, ambaye jina lake alikuwa Yohana. [7] Alikuja
kama shahidi kushuhudia kuhusu ile nuru, ili kwamba wote waweze kuamini kupitia
yeye. [8] Yohana hakuwa ile nuru, bali alikuja ili ashuhudie kuhusu ile nuru [9] Hiyo
ilikuwa nuru ya kweli ambayo ilikuwa inakuja katika dunia nayo humtia nuru
kila mmoja [10] Alikuwa katika dunia, na dunia iliumbwa kupitia yeye, na dunia
haikumjua. [11] Alikuja kwa vitu vyake, na watu wake hawakumpokea. [12] Bali kwa
wale wengi waliompokea, ambao waliamini jina lake, kwa hao aliwapa haki ya
kuwa wana wa Mungu, [13] Ambao walizaliwa, sio kwa damu, wala kwa mapenzi
ya mwili, wala kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu mwenyewe. [14] Naye Neno
alifanyika mwili na akaishi miongoni mwetu, tumeuona utukufu wake, utukufu
kama wa mtu pekee wa kipekee aliyekuja kutoka kwa Baba, amejaa neema na
kweli. [15] Yohana alishuhudia kuhusu yeye, na alipaza sauti akisema, “Huyu ndiye
ambaye nilisema habari zake nikisema, “Yule ajaye baada yangu ni mkuu kuliko
mimi, kwa sababu amekuwako kabla yangu.” [16] Kwa kuwa kutoka katika utimilifu
wake, sisi sote tumepokea bure kipawa baada ya kipawa. [17] Kwa kuwa sheria ililetwa
kupitia Musa. Neema na kweli vilikuja kupitia Yesu Kristo. [18] Hakuna mwanadamu
aliyemwona Mungu wakati wowote. Mtu pekee ambaye ni Mungu, aliye katika
kifua cha Baba, amemfanya yeye ajulikane. [19] Na huu ndio ushuhuda wa Yohana
wakati makuhani na walawi waliotumwa kwake na Wayahudi kumwuliza, “Wewe
ni nani?” [20] Bila kusitasita na hakukana, bali alijibu, “Mimi sio Kristo.” [21] Hivyo
wakamuuliza, “kwa hiyo wewe ni nani sasa?” Wewe ni Eliya? Akasema, “Mimi siye.”
Wakasema, Wewe ni nabii? Akajibu,” Hapana.” [22] Kisha wakamwambia, “Wewe ni
nani, ili kwamba tuwape jibu waliotutuma”? Wajishuhudiaje wewe mwenyewe?”
[23] Akasema, “Mimi ni sauti yake aliaye nyikani: 'Inyosheni njia ya Bwana,' kama
nabii Isaya alivyosema.” [24] Basi kulikuwa na watu wametumwa pale kutoka kwa
Mafarisayo. Wakamuuliza na kusema, [25] “Kwa nini unabatiza basi kama wewe
sio Kristo wala Eliya wala nabii?” [26] Yohana aliwajibu akisema, “Ninabatiza kwa
maji. Hata hivyo, miongoni mwenu anasimama mtu msiyemtambua. [27] Huyu ndiye
ajaye baada yangu. Mimi sisitahili kulegeza kamba za viatu vyake.” [28] Mambo
haya yalitendeka huko Bethania, ng'ambo ya Yordani, mahali ambapo Yohana
alikuwa akibatiza. [29] Siku iliyofuata Yohana alimwona Yesu akija kwake akasema,
“ Tazama mwanakondoo wa Mungu aichukuae dhambi ya ulimwengu! [30] huyu
ndiye niliyesema habari zake nikisema, “Yeye ajaye nyuma yangu ni mkuu kuliko
mimi, kwa kuwa alikuwa kabla yangu.' [31] Sikumtambua yeye, lakini ilifanyika
hivyo ili kwamba afunuliwe katika Israeli, kwamba nilikuja nikibatiza kwa maji.”
[32] Yohana alishuhudia, “Niliona Roho akishuka kutoka mbinguni mfano wa hua, na
ilibaki juu yake. [33] Mimi sikumtambua lakini yeye aliyenituma ili nibatize kwa maji
aliniambia, 'yule ambaye utaona Roho akishuka na kukaa juu yake, Huyo ndiye
abatizaye kwa Roho Mtakatifu.' [34] Nimeona na nimeshuhudia kwamba huyu ni
Mwana wa Mungu.” [35] Tena siku iliyofuata Yohana alikuwa amesimama pamoja
na wanafunzi wake wawili, [36] walimwona Yesu akitembea na Yohana akasema,

“Tazama, Mwana kondoo wa Mungu!” 37 Wanafunzi wawili walimsikia Yohana
akisema haya wakamfuata Yesu. 38 Tena Yesu aligeuka na kuwaona wanafunzi
wale wakimfuata, na akawambia, “Mnataka nini?” Wakajibu, “Rabbi, (maana yake
'mwalimu,' unaishi wapi?” 39 Akawambia, “Njooni na mwone.”Kisha walikwenda
na kuona mahali alipokuwa akiishi; walikaa pamoja naye siku hiyo, kwa kuwa
ilikuwa yapata kama saa kumi hivi. 40 Mmoja wa wale wawili waliomsikia Yohana
akiongea na kisha kumfuata Yesu alikuwa ni Andrea, ndugu yake Simoni Petro.
41 Akamwona ndugu yake Simoni na akamwambia, “Tumempata Masihi” (ambayo
inatafsiriwa Kristo). 42 Akamleta kwa Yesu. Yesu akamtazama na akasema, “Wewe
ni Simoni mwana wa Yohana” utaitwa Kefa,” (maana yake 'Petro'). 43 Siku iliyofuata
wakati Yesu alipotaka kuondoka kwenda Galilaya, alimpata Filipo na akamwambia,
“Nifuate mimi.” 44 Filipo alikuwa ni mwenyeji wa Bethsaida, mji wa Andrea na
Petro. 45 Filipo alimpata Nathanaeli na kumwambia, Tumempata yule ambaye Musa
aliandika habari zake katika sheria na Manabii. Yesu mwana wa Yusufu, kutoka
Nazareti. 46 Nathanaeli akamwambia, “Je kitu chema chaweza kutokea Nazareti?”
Filipo akamwambia, Njoo na uone.” 47 Yesu akamwona Nathanaeli akija kwake
na akasema, “Tazama, Mwisraeli kweli kweli asiye na udanganyifu ndani yake!”
48 Nathanaeli akamwambia, “Umenifahamuje mimi?” Yesu akajibu na akamwambia,
“Kabla Filipo hajakuita ulipokuwa chini ya mtini, nalikuona.” 49 Nathanaeli akajibu,
“Rabi wewe u Mwana wa Mungu! Wewe ni Mfalme wa Israeli”! 50 Yesu akajibu
akamwambia, Kwa sababu nilikuambia 'nilikuona chini ya mtini' je waamini? utaona
matendo makubwa kuliko haya.” 51 Yesu akasema, “Amini amini nawambieni
mtaziona mbingu zikifunguka, na kuwaona malaika wakipanda na kushuka juu ya
Mwana wa Adamu.”

# 2

1 Baada ya siku tatu, kulikuwa na arusi huko Kana ya Galilaya na mama yake
Yesu alikuwa huko. 2 Yesu na wanafunzi wake walikuwa wamealikwa katika
arusi. 3 Wakati walipoishiwa na divai, mama yake Yesu akamwambia, “Hawana
divai.” 4 Yesu akajibu, “Mwanamke hiyo inanihusu nini mimi? Muda wangu mimi
bado haujatimia.” 5 Mama yake akawambia watumishi, “Chochote atakachowambia
fanyeni.” 6 Basi kulikuwa na mitungi sita ya mawe pale iliyowekwa kwa ajili
ya kunawa katika sikukuu za Wayahudi, kila moja lilikuwa na ujazo wa nzio
mbili tatu. 7 Yesu akawambia, “Ijazeni maji mitungi ya mawe.” Wakajaza hadi
juu. 8 Kisha akawambia wale watumishi, “Chukueni kiasi sasa na mpeleke kwa
muhudumu mkuu wa meza.” Wakafanya kama walivyoagizwa. 9 Mhudumu mkuu
aliyaonja yale maji yaliyokuwa yamebadilika na kuwa divai, ila hakujua yalikotoka
(lakini watumishi waliochota maji walijua yalikotoka). Kisha akamwita bwana
harusi na 10 kumwambia, “Kila mmoja huanza kuwahudumia watu divai nzuri na
wakiishalewa huwapa divai isiyo nzuri. Lakini wewe umeitunza divai nzuri hadi
sasa” 11 Muujiza huu wa Kana ya Galilaya, ulikuwa ndio mwanzo wa ishara za miujiza
aliyoifanya Yesu, akifunua utukufu wake, hivyo wanafunzi wake wakamwamini.
12 Baada ya hii, Yesu, mama yake, ndugu zake na wanafunzi wake walienda katika mji
wa Kapernaum na wakaa huko kwa siku chache. 13 Basi Pasaka ya Wayahudi ilikuwa
imekaribia, hivyo Yesu akaenda Yerusalemu. 14 Akawakuta wauzaji wa ng'ombe,
kondoo, na njiwa ndani ya Hekalu. Pia na wabadilisha fedha walikuwa wameketi
ndani ya Hekalu. 15 Yesu akatengeneza mjeledi wenye vifundo, akawatoa wote
walikuwemo katika hekalu, ikijumuisha ng'ombe na kondoo. Akamwaga fedha za
wabadili fedha na kuzipindua meza zao. 16 Kwa wauzaji wa njiwa akawambia, “Toeni
vitu hivi mbali na mahali hapa, acheni kuifanya nyumba ya Baba yangu kuwa mahali

pa soko.” 17 Wanafunzi wake wakakumbuka kuwa ilikuwa imeandikwa, “Wivu wa
nyumba yako utanila.” 18 Wakuu wa Kiyahudi wakajibu, wakamwambia, Ni ishara
ipi utakayoionyesha kwa sababu unayafanya mambo haya?” 19 Yesu akawajibu,
libomoeni Hekalu hili nami nitalijenga baada ya siku tatu.” 20 Kisha wakuu wa
Wayahudi wakasema, “Iligharimu miaka arobaini na sita kujenga hekalu hili nawe
unasema utalijenga kwa siku tatu?” 21 Ingawa, yeye aliongea hekalu akimaanisha
mwili wake. 22 Hivyo baadaye baada ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu, wanafunzi
wake wakakumbuka kuwa alisema hivyo, wakaamini maandiko na kauli hii ambayo
Yesu alikuwa amekwisha kuisema. 23 Basi alipokuwa Yerusalemu wakati wa Pasaka,
wakati wa sikukuu watu wengi waliamini jina lake, walipoona ishara ya miujiza
aliyoifanya. 24 Lakini Yesu hakuwa na imani nao kwa sababu aliwajua wanadamu
wote. 25 Hakuhitaji mtu yeyote kumwambia kuhusu walivyo wanadamu kwa sababu
alijua kilichokuwamo ndani yao.

# 3

1 Basi kulikuwa na Farisayo ambaye jina lake Nikodemo, mmoja wa wajumbe wa
baraza la Wayahudi. 2 Mtu huyu alimwendea Bwana Yesu usiku na akamwambia,
“Rabi, tunajua ya kuwa u mwalimu kutoka kwa Mungu, kwa maana hakuna mtu
awezaye kutenda ishara hizi zote Mungu asipokuwa pamoja naye.” 3 Yesu akamjibu,
“Amini, amini, mtu hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu asipozaliwa mara
ya pili.” 4 Nikodemo akasema,” Mtu anawezaje kuzaliwa akiwa mzee? Hawezi
kuingia tumboni mwa mama yake mara ya pili na kuzaliwa, je anaweza?” 5 Yesu
akajibu, “Amini, amini mtu sipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia
katika ufalme wa Mungu. 6 Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili, na kilichozaliwa kwa
Roho ni roho. 7 Usishangae kwa sababu nilikuwambia, 'ni lazima kuzaliwa mara
ya pili.' 8 Upepo huvuma popote upendapo na sauti yake mwaisikia, lakini hamjui
utokako wala uendako. Ndivyo ilivyo hali ya kila aliyezaliwa na roho. 9 Nikodemo
akajibu, kwa kusema, “Mambo haya yawezekanaje?” 10 Yesu akamjibu, “Wewe u
mwalimu wa Israeli, hata hauyajui mambo haya? 11 Amini, amini, nakuambia, kile
tunachokifahamu twakishuhudia kwa kile tulichokiona. Lakini hampokei ushuhuda
wetu. 12 Kama nimewambia mambo ya hapa duniani na hamuamini, mtawezaje
kuamini kama nikiwambia mambo ya mbinguni? 13 Maana hakuna aliyepanda juu
kutoka mbinguni isipokuwa yeye aliyeshuka, Mwana wa Adamu. 14 Kama vile Musa
alivyomwinua nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu lazima ainuliwe, 15 ili
kwamba wote watakaomwamini wapate uzima wa milele. 16 Kwa maana jinsi hii
Mungu aliupenda ulimwengu, kwamba akamtoa mwanae wa pekee, ili kwamba mtu
yeyote amwaminiye asiangamie bali awe na uzima wa milele. 17 Kwa sababu Mungu
hakumtuma mwanae duniani ili auhukumu ulimwengu, bali kwamba ulimwengu
uokolewe katika yeye. 18 Amwaminiye Yeye hatahukumiwa. Yeye asiyemwamini
tayari ameshahukumiwa kwa sababu hajaliamini jina la Mwana pekee wa Mungu.
19 Hii ndiyo sababu ya hukumu, ya kwamba nuru imekuja ulimwenguni, lakini
wanadamu wakapenda giza zaidi ya nuru kwa sababu matendo yao yalikuwa maovu.
20 kila mtu atendaye mabaya huichukia nuru wala haji nuruni ili matendo yake yasije
yakawekwa wazi. 21 Lakini, yeye atendaye kweli huja kwenye nuru ili matendo
yake yaonekane kwamba yametendwa kwa utiifu wa Mungu. 22 Baada ya haya,
Yesu pamoja na wanafunzi walienda katika nchi ya Yudea. Huko alitumia muda
pamoja nao na alikuwa akibatiza. 23 Sasa Yohana pia alikuwa akibatiza huko Ainea
karibu na Salim maana kulikuwa na maji mengi pale. Watu walikuwa wakija kwake
na kubatizwa, 24 kwa kuwa Yohana alikuwa hajatupwa gerezani. 25 Kisha palitokea
mabishano kati ya wanafunzi wa Yohana na Myahudi kuhusu sikukuuu za utakaso.

[26] Wakaenda kwa Yohana wakamwambia, “Rabi, yeye uliyekuwa naye ng'ambo ya
Mto Yorodani, yeye uliyeshuhudia habari zake, tazama, anabatiza na wote wanaenda
wanamfuata.” [27] Yohana akajibu mtu hawezi kupokea kitu chochote isipokuwa kama
amepewa kutoka mbinguni. [28] Ninyi wenyewe mwashuhudia kuwa nalisema kuwa,
'mimi sio Kristo', badala yake nilisema, 'nimetumwa mbele yake.' [29] Yeye aliye na
bibi arusi ni bwana harusi. Sasa rafiki wa bwana arusi, asimamaye na kusikiliza
hufurahia sana kwa sababu ya sauti ya bwana arusi. Hii sasa ni furaha yangu
iliyotimilika. [30] Anapaswa kuzidi, nami napaswa kupungua. [31] Yeye atokaye juu,
yu juu ya yote. Yeye aliye wa ulimwengu anatoka ulimwenguni na huongea mambo
ya ki ulimwengu. Yeye atokaye mbinguni yuko juu ya yote. [32] Yeye hushuhudia
yale aliyoyaona na kuyasikia, lakini hakuna apokeaye ushuhuda wake. [33] Yeye aliye
pokea ushuhuda wake amehakikisha kuwa Mungu ni mkweli. [34] Kwa sababu yeye
aliyetumwa na Mungu huongea maneno ya Mungu. Kwa kuwa hampi Roho kwa
kipimo. [35] Baba humpenda Mwana na amempa vitu vyote mikononi mwake. [36] Yeye
amwaminiye Mwana anao uzima wa milele, lakini kwa yeye asiye mtii Mwana
hatauona uzima, bali ghadhabu ya Mungu hushikamana juu yake.

# 4

[1] Basi Yesu alipofahamu kuwa Mafarisayo wamesikia kuwa Yesu alikuwa anafuasa
na kuwabatiza zaidi ya Yohana, [2] (ingawa Yesu mwenyewe alikuwa habatizi ila
wanafunzi wake), [3] alitoka Judea na akaenda Galilaya. [4] Hivyo ilikuwa muhimu
kupitia Samaria. [5] Na akafika kwenye mji wa Samaria, unaoitwa Sikari, karibu na
eneo ambalo Yakobo alimpa mwanae Yusufu. [6] Na kisima cha Yakobo kilikuwa hapo.
Yesu alikuwa amechoka kwa ajili ya safari na akakaa karibu na kisima. Ilikuwa muda
wa mchana. [7] Mwanamke Msamaria alikuja kuteka maji, na Yesu akamwambia,
“Nipe maji ninywe.” [8] Kwa sababu wanafunzi wake walikuwa wameenda zao
mjini kununua chakula. [9] Yule mwanamke akamwambia, “Inakuaje wewe Myahudi,
kuniomba mimi mwanamke Msamaria, kitu cha kunywa?” Kwa sababu Wayahudi
hawachangamani na Wasamaria. [10] Yesu akamjibu, “Kama ungelijua karama ya
Mungu, na yule anayekuambia 'Nipe maji, ' ungelimwomba, na angelikupa maji
ya uzima.” [11] Mwanamke akajibu, “Bwana hauna ndoo ya kuchotea, na kisima ni
kirefu. Utayapata wapi Maji ya Uzima.? [12] Je wewe ni mkuu, kuliko baba yetu
Yakobo, ambaye alitupa kisima hiki, na yeye mwenyewe na watoto wake pamoja na
mifugo yake wakanywa maji ya kisima hiki?” [13] Yesu akajibu, “Yeyote anywae maji
haya atapata kiu tena, [14] lakini yeye atakaye kunywa maji nitakayompa hatapata
kiu tena. Badala yake maji nitakayompa yatakuwa chemchemi inayobubujika hata
milele.” [15] Yule mwanamke akamwambia, “Bwana, nayaomba maji hayo ili nisipate
kiu, na nisihangaike kuja hapa kuchota maji.” [16] Yesu akamwambia, “Nenda kamwite
mumeo, kisha urudi.” [17] Mwanamke akamwambia, “Sina mume.” Yesu akajibu,
“Umesema vyema, 'Sina mume;' [18] kwa maana umekuwa na wanaume watano,
na mmoja ambaye unaye sasa sio mume wako. Katika hili umesema kweli!”
[19] Mwanamke akamwambia, “Bwana naona yakuwa wewe ni nabii. [20] Baba zetu wali-
abudu katika mlima huu. Lakini ninyi mwasema ya kuwa Yerusalemu ndiyo sehemu
ambayo watu wanapaswa kuabudu.” [21] Yesu akamjibu, “Mwanamke, niamini, wakati
unakuja ambapo hamtamwabudu Baba katika mlima huu au Yerusalemu. [22] Ninyi
watu mwaabudu kile msichokijua, lakini sisi twaabudu tunachokijua, kwa sababu
wokovu watoka kwa Wayahudi.” [23] Hatahivyo, wakati unakuja, na sasa upo hapa,
wakati waabuduo kweli watamwabudu Baba katika roho na kweli, kwa sababu Baba
anawatafuta watu wa namna hiyo kuwa watu wake wanao mwabudu. [24] Mungu
ni Roho, na wale wanaomwabudu wanapaswa kumwabudu kwa roho na kweli.”

[25] Mwanamke akamwambia, “Ninajua kuwa Masihi anakuja, (aitwaye Kristo). Huyo
atakapokuja atatwambia yote.” [26] Yesu akamwambia, “Mimi unayesema nami ndiye.”
[27] Wakati huo huo wanafunzi wake wakarudi. Nao walishangaa kwa nini alikuwa
akizungumza na mwanamke, lakini hakuna aliyethubutu kumuuliza, “Unataka nini?”
au “Kwa nini unazungumza naye.?” [28] Hivyo mwanamke akauacha mtungi wake na
akaenda mjini na akawambia watu, [29] “Njooni mwone mtu aliyeniambia mambo
yangu yote niliyoyatenda, je yawezekana akawa ndiye Kristo?” [30] Wakatoka mjini
wakaja kwake. [31] Wakati wa mchana wanafunzi wake walimsihi wakisema, “Rabi
kula chakula.” [32] lakini yeye aliwambia, “Mimi ninacho chakula msichokijua ninyi.”
[33] Wanafunzi wakaambizana, hakuna aliyemletea kitu chochotekula,”Je walileta?”
[34] Yesu akawambia, “Chakula changu ni kufanya mapenzi yake yeye aliyenituma
na kutimiza kazi yake. [35] Je, hamsemi, 'Bado miezi mitano na mavuno yatakuwa
tayari?' Ninawambieni tazameni mashamba yalivyo tayari kwa mavuno! [36] Yeye
avunaye hupokea mishahara na kukusanya matunda kwa ajili ya uzima wa milele,
ili kwamba yeye apandaye naye avunaye wafurahi pamoja. [37] Kwa kuwa msemo
huu ni wa kweli, 'Mmoja apanda na mwingine avuna.' [38] Niliwatuma kuvuna
ambacho hamkukihangaikia, Wengine wamefanya kazi na ninyi mmeingia katika
furaha ya kazi yao.” [39] Wasamaria wengi katika mji ule walimwani kwa sababu
ya taarifa ya yule mwanamke aliyekuwa akishuhudia, “Aliyeniambia mambo yote
niliyoyafanya.” [40] Hivyo Wasamaria walipokuja walimsihi akae pamoja nao na
akakaa kwao kwa siku mbili. [41] Na wengi zaidi wakamwamini kwa sababu ya neno
lake. [42] Wakamwambia yule mwanamke, “Tunaamini sio tu kwa maneno yako, kwa
sababu sisi wenyewe tumesikia, na sasa twafahamu kuwa hakika yeye ni mwokozi
wa ulimwengu.” [43] Baada ya siku hizo mbili, akaondoka na kuelekea Galilaya.
[44] Kwa sababu yeye mwenyewe alikuwa ametangaza kuwa nabii hana heshima katika
nchi yake mwenyewe. [45] Alipokuja kutoka Galilaya, Wagalilaya walimkaribisha.
Walikuwa wameona mambo yote aliyoyafanya Yerusalemu kwenye sikukuu, kwa
sababu na wao pia walikuwa wamehudhuria kwenye sikukuu. [46] Alikuja tena Kana
ya Galilaya huko alikoyabadilisha maji kuwa divai. Palikuwa na ofisa ambaye mwana
wake alikuwa ni mgonjwa huko Kapernaumu. [47] Aliposikia kuwa Yesu alitoka Judea
na kwenda Galilaya, alienda kwa Yesu na kumsihi atelemke amponye mwanawe,
ambaye alikuwa karibu kufa. [48] Ndipo Yesu akamwambia, “Ninyi msipoona ishara
na maajabu hamwezi kuamini. [49] Kiongozi akasema, “ Bwana shuka chini kabla
mwanangu hajafa.” [50] Yesu akamwambia, “Nenda mwanao ni mzima.” Yule mtu
akaamini neno alilolisema Yesu na akaenda zake. [51] Alipokuwa akishuka, watumishi
wake walimpokea na kumwambia mwana wake alikuwa mzima. [52] Hivyo akawauliza
ni muda gani alipata nafuu. Wakajibu, “Jana muda wa saa saba homa ilipomwacha.”
[53] Ndipo baba yake akatambua kuwa ni muda ule ule Yesu aliosema, “Mwana wako
ni mzima.” Hivyo yeye na familia yake wakaamini. [54] Hii ilikuwa ni ishara ya pili
aliyoifanya Yesu alipotoka Yudea kwenda Galilaya.

# 5

[1] Baada ya hapo kulikuwa na sikukuu ya Wayahudi, na Yesu alipanda kwenda
Yerusalemu. [2] Na kule Yerusalemu palikuwa na birika kwenye mlango wa kondoo,
lililokuwa likiitwa kwa lugha ya Kiebrania Bethzatha, nalo lina matao matano.
[3] Idadi kubwa ya wagonjwa ilikuwemo, vipofu, viwete, au waliopooza walikuwa
wamelala katika matao hayo. {Zingatia: Maneno ya mstari wa 3 hayaonekani katika
nakala nzuri za kale. “Wakisubiri maji kutibuliwa.”) Kwa hakikia wakati fulani
malaika alishuka ndani ya Bwana na kuyatibua maji. [4] Kwahiyo, yule ambaye
alikuwa wa kwanza kuingia ndani ya baada ya maji kutibuliwa alifanywa mzima

kutokana na chochote kilichokuwa kimemshika kwa wakati huo. 5 Na mtu mmoja
aliyekuwa ameugua kwa muda wa miaka thelathini na minane alikuwa ndani
ya matao. 6 Yesu alipomwona amelala ndani ya matao na baada ya kutambua
kuwa amelala pale kwa muda mrefu Yesu alimwambia, “Je unataka kuwa mzima?”
7 Yule mgonjwa akamjibu, “Bwana sina mtu, wa kuniweka katika birika wakati
maji yanapotibuliwa. Wakati ninapojaribu kuingia mtu mwingine hunitangulia.”
8 Yesu akamwambia, “Inuka na uchukue godoro lako na uende.” 9 Mara yule mtu
akaponywa, akachukua kintanda chake na akaenda. Na siku hiyo ilikuwa siku ya
Sabato. 10 Hivyo Wayahudi wakamwambia yule mtu aliyeponywa, “Leo ni siku ya
Sabato, na hauruhusiwi kubeba godoro lako.” 11 Akajibu, yeye aliyeniponya ndiye
aliyeniambia, “Chukua godoro lako na uende.” 12 Wakauliza, “Ni nani aliyekuambia
'Chukua godoro lako na uende?"' 13 Ingawa, yule aliyeponywa hakumjua, kwa sababu
Yesu alikuwa ameondoka kwa siri. Kwa kuwa kulikuwa na watu wengi katika
sehemu hiyo. 14 Baada ya hapo Yesu alimkuta yule mtu hekaluni na akamwambia,
“Tazama, umepona! “Usitende dhambi tena usije ukapatwa na jambo baya zaidi.”
15 Yule mtu akaenda na kuwataarifu Wayahudi kuwa Yesu ndiye aliyemponya.
16 Hivyo, kwa sababu ya mambo hayo Wayahudi walimtesa Yesu, kwa sababu alifanya
mambo haya siku ya Sabato. 17 Yesu akawambia, “Baba yangu anafanya kazi
hata sasa nami nafanya kazi.” 18 Kwa sababu hiyo Wayahudi walizidi kumtafuta
ili wamuue sio tu kwa sababu ya kuivunja Sabato, bali kwa kumwita Mungu
Baba yake, akijifanya kuwa sawa na Mungu. 19 Yesu akawajibu, “Amini, amini,
Mwana hawezi kufanya kitu chochote isipokuwa kile ambacho amemwona Baba yake
anakifanya, kwa kuwa chochote Baba akifanyacho ndicho na Mwana atakachofanya.
20 Kwa kuwa Baba ampenda Mwana, na amwonyesha kila kitu anachokifanya na
atamwonyesha mambo makubwa kuliko haya ili kwamba mzidi kushangaa.” 21 Kwa
kuwa kama vile ambavyo Baba awafufuavyo wafu na kuwapa uzima, halikadhalika
Mwana pia humpa yeyote ampendaye. 22 Kwa kuwa Baba hamhukumu yeyote,
bali amempa Mwana hukumu yote 23 ili kwamba wote wamuheshimu Mwana kama
vile Mwana anavyomuheshimu Baba. Yeye asiyemuheshimu Mwana hamuheshimu
Baba aliyemtuma. 24 Amini, amini, yeye asikiaye neno langu na kumwamini yeye
aliyenituma anao uzima wa milele na hatahukumiwa. Badala yake, amepita kutoka
mautini na kuingia uzimani. 25 Amini, amini, nawambia wakati unakuja na sasa
upo ambao wafu watasikia sauti ya Mwana wa Mungu, na wote watakao sikia
wataishi. 26 Kwa kuwa kama vile Baba alivyo na uzima ndani yake mwenyewe,
27 kadhalika amempa Mwana kuwa na uzima ndani yake, na Baba amempa Mwana
mamlaka ili kwamba ahukumu kwa kuwa ni Mwana wa Adamu. 28 Msishangazwe
na hili, kwa kuwa wakati unakuja ambao wafu wote waliomo makaburini wataisikia
sauti yake 29 nao watatoka nje: kwa waliotenda mema kwa ufufuo wa uzima, na
walio tenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu. 30 Siwezi kufanya kitu chochote
kutoka kwangu mwenyewe. Kama nisikiavyo, ndivyo ninavyo hukumu na hukumu
yangu ni ya haki kwa kuwa sitafuti mapenzi yangu, bali mapenzi yake aliyenituma.
31 Kama nikijishuhudia mwenyewe, ushuhuda wangu usingelikuwa wa kweli.
32 Kuna mwingine anayeshuhudia kuhusu mimi na ninajua kwa hakika ushuhuda
anaonishuhudia ni wa kweli. 33 Mmetuma kwa Yohana naye ameishuhudia kweli.
34 Hatahivyo, ushuhuda ninaoupokea hautoki kwa mwanadamu. Ninayasema haya ili
kwamba mweze kuokolewa. 35 Yohana alikuwa ni taa iliyokuwa ikiwaka na kung'ara,
na mlikuwa tayari kuifurahia kwa muda kitambo nuru yake. 36 Ushuhuda nilionao
ni mkuu kuliko ule wa Yohana, kwa kazi ambazo Baba amenipa kuzikamilisha,
hizo kazi nizifanyazo zashuhudia kuwa Baba amenituma. 37 Baba aliyenituma yeye
mwenyewe ameshuhudia kuhusu mimi. Hamjawahi kusikia sauti yake wala kuona

umbo lake wakati wowote. 38 Hamna neno lake likikaa ndani yenu kwa kuwa
hamumwamini yeye aliyetumwa. 39 Mnayachunguza maandiko mkidhani ndani yake
mna uzima wa milele, na hayo maandiko yanashuhudia habari zangu na 40 hamtaki
kuja kwangu ili mpate uzima wa milele. 41 Sipokei sifa kutoka kwa watu, 42 lakini
ninajua kuwa hamna upendo wa Mungu ndani yenu ninyi wenyewe. 43 Nimekuja
kwa jina la Baba yangu, hamukuweza kunipokea. Kama mwingine akija kwa jina lake
mngempokea. 44 Je mnawezaje kuamini ninyi ambao mnapokea sifa kutoka kwa kila
mmoja wenu lakini hamtafuti sifa itokayo kwa Mungu wa pekee? 45 Msidhani mimi
nitawashitaki mbele za Baba. Anayewashitaki ninyi ni Musa, ambaye ninyi mmeweka
matumaini yenu kwake. 46 Kama mngekuwa mnamwamini Musa, mngeniamini mimi
kwa sababu aliandika kuhusu habari zangu. 47 Kama hamuamini maandiko yake,
mtawezaje kuamini maneno yangu.?

# 6

1 Baada ya mambo haya, Yesu alienda pande za Bahari ya Galilaya, pia huitwa
Bahari ya Tiberia. 2 Mkutano mkubwa ulikuwa ukimfuata kwa sababu waliona
ishara alizozifanya kwa waliokuwa wagonjwa. 3 Yesu alipanda juu hadi upande
wa juu wa mlima na akakaa huko na wanafunzi wake 4 (Na Pasaka, Sikukuu
ya Wayahudi ilikuwa imekaribia). 5 Yesu alipoinua macho yake juu na kuona
umati mkubwa unakuja kwake, akamwambia Filipo, “Tutakwenda wapi kununua
mikate ili hawa waweze kula”? 6 (Lakini Yesu aliyasema haya kwa Filipo kwa
kumjaribu kwa kuwa yeye mwenyewe alijua atakachofanya). 7 Filipo akamjibu,
“Hata mikate ya thamani ya dinari mia mbili isingelitosha hata kila mmoja kupata
hata kipande kidogo.” 8 Andrea, mmoja wa wanafunzi wake ndugu yake Simoni
Petro akamwambia 9 Yesu, “Kuna mvulana hapa ana mikate mitano na samaki
wawili, lakini hii yafaa nini kwa watu wengi namna hii?” 10 Yesu akawambia,
“Waketisheni watu chini” (kulikuwa na nyasi nyingi mahali pale). Hivyo wanaume
wapata elfu tano wakakaa chini. 11 Kisha Yesu akachukua ile mikate mitano
akashukuru akawawagawia wale waliokuwa wamekaa. Vivyo hivyo akawagawia
samaki kwa kadiri ya vile wavyohitaji. 12 Watu waliposhiba, aliwambia wanafunzi
wake, “Vikusanyeni vipande vya mabaki, vilivyobaki ili kwamba kisipotee chochote.”
13 Basi wakakusanya na kujaza vikapu kumi na viwili, vipande vya mikate mitano
ya shayiri- vipande vilivyosazwa na wale waliokula. 14 Kisha watu walipoona
ishara hii aliyoifanya walisema, “Kweli huyu ndiye yule nabii ajaye ulimwenguni.”
15 Yesu alipotambua kuwa walikuwa wanataka kumkamata ili wamfanye kuwa
mfalme wao, alijitenga, tena na akaenda mlimani yeye peke yake. 16 Ilipokuwa
jioni, wanafunzi wake walishuka kwenda ziwani. 17 Wakapanda kwenye mtumbwi
na walikuwa wakivuka kuelekea Kapernaumu. (Giza lilikuwa limeingia na Yesu
alikuwa bado hajaja kwao). 18 Wakati huo upepo mkali ulikuwa ukivuma, na
bahari ilikuwa ikendelea kuchafuka. 19 Tena wanafunzi wake walipokuwa wamepiga
makasia kama ishirini na matano au thelathini, wakamwona Yesu akitembea
juu ya bahari kuukaribia mtumbwi, na wakaogopa. 20 Lakini akawambia, “Ni
mimi! Msiogope.” 21 Tena walikuwa tayari kumbeba kwenye mtumbwi, na mara
mtumbwi ulifika kwenye nchi mahali walipokuwa wakienda. 22 Siku iliyofuata,
mkutano uliokuwa umesimama upande wa bahari waliona kuwa hakuna mtumbwi
mwingine isipokuwa ule ambayo Yesu na wanafunzi wake walikuwa hawajaupanda
lakini wanafunzi wake walikuwa wameenda zao wenyewe. 23 (Ingawa, kulikuwa
na baadhi ya mitumbwi iliyotoka Tiberia karibu na mahali walipokula mikate
baada ya Bwana kutoa shukrani). 24 Wakati makutano walipotambua kuwa sio
Yesu wala wanafunzi wake walikuwa kule, wao wenyewe walipanda ndani ya

mitumbwi wakaenda Kapernaumu wakimtafuta Yesu. 25 Baada ya kumpata upande
mwingine wa ziwa wakamuuliza, “Rabbi ulikuja lini huku?” 26 Yesu akawajibu,
akawambia, Amini, amini, mnanitafuta mimi, sio kwa sababu mliziona ishara,
bali kwa sababu mlikula mikate na kushiba. 27 Acheni kukifanyia kazi chakula
chenye kuharibika, bali mkifanyie kazi chakula kidumucho hata milele kile ambacho
mwana wa Adamu atawapa, kwa kuwa Mungu Baba ameweka muhuri juu yake.”
28 Kisha wakamwambia, “Ni nini tunapaswa kufanya ili kuzifanya kazi za Mungu?”
29 Yesu akajibu, “Hii ndiyo kazi ya Mungu: kwamba mmwamini yeye aliyemtuma.”
30 Basi wakamwambia, “Ni ishara zipi utakazofanya, kwamba tunaweza kuziona na
kukuamini? Utafanya nini? 31 Baba zetu walikula manna jangwani, kama ilivyo
andikwa, “Aliwapa mikate kutoka mbinguni ili wale.” 32 Kisha Yesu akawajibu,
“Amini, amini, sio Musa aliyewapa mkate kutoka mbinguni, bali Baba yangu ndiye
awapaye mkate wa kweli kutoka mbinguni. 33 Kwa kuwa mkate wa Mungu ni ule
ushukao kutoka mbinguni na kuupatia uzima ulimwengu. 34 Basi wakamwambia,
“Bwana tupatie huu mkate wakati wote.” 35 Yesu akawambia, “Mimi ndiye mkate
wa uzima, yeye ajaye kwangu hatapata njaa na yeye aniaminiye hatahisi kiu
kamwe.” 36 Ingawa niliwaambia kwamba, mmeniona, na bado hamuamini. 37 Wote
ambao Baba anaonipa watakuja kwangu, na yeyote ajaye kwangu sitamtupa nje
kabisa. 38 Kwa kuwa nimeshuka kutoka mbinguni, sio kwa ajili ya kufanya mapenzi
yangu, bali mapenzi yake aliyenituma. 39 Na haya ndiyo mapenzi yake aliyenituma,
kwamba nisimpoteze hata mmoja wa wale alionipa, bali nitawafufua siku ya mwisho.
40 Kwa kuwa haya ndiyo mapenzi ya Baba yangu, kwamba yeyote amtazamaye
Mwana na kumwamini apate uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho.
41 Kisha wayahudi wakamnung`unikia kumhusu yeye kwa sababu alisema, “Mimi
ni mkate ulioshuka kutoka mbinguni.” 42 Wakasema, “Huyu siyo Yesu mwana wa
Yusuph, ambaye baba yake na mama yake tunamfahamu? Imekuwaje sasa anasema,
'Nimeshuka kutoka mbinguni`?” 43 Yesu akajibu, akawambia, “Msinung'unikiane
miongoni mwenu wenyewe. 44 Hakuna mtu ajaye kwangu asipovutwa na Baba
yangu aliyenituma, nami nitamfufua siku ya mwisho. 45 Kwa kuwa imeandikwa
katika manabii, 'Watafundishwa na Mungu.' Kila aliyesikia na amejifunza kutoka
kwa Baba, huja kwangu. 46 Sio kwamba kuna mtu aliyemwona Baba, isipokuwa yeye
atokaye kwa Mungu- amemwona Baba. 47 Amini, amini yeye aaminiye anao uzima
wa milele. 48 Mimi ni mkate wa uzima. 49 mababa zenu walikula manna jangwani, na
wakafa. 50 Huu ndio mkate ushukao kutoka mbinguni, ili kwamba mtu aule sehemu
yake ili asife. 51 Mimi ni mkate uishio ambao umeshuka kutoka mbinguni. Kama
mtu yeyote akila sehemu ya mkate huu, ataishi milele. Mkate nitakao utoa ni mwili
wangu kwa ajili ya uzima wa ulimwengu.” 52 Wayahudi wakakasirika wenyewe kwa
wenyewe na wakaanza kubishana wakisema, “Mtu huyu anawezaje kutupa mwili
wake tuule?” 53 Kisha Yesu akawambia, “Amini, amini, msipoula mwili wa Mwana
wa Adamu na kuinywa damu yake, hamta kuwa na uzima ndani yenu. 54 Yeyote
aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele, nami nitamfufua
siku ya mwisho. 55 Kwa kuwa mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu
ni kinywaji cha kweli. 56 Yeye aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa
ndani yangu, nami ndani yake. 57 Kama Baba mwenye uzima alivyonituma, na kama
niishivyo kwa sababu ya Baba, na yeye pia ataishi kwa sababu yangu. 58 Huu ndio
mkate ushukao kutoka mbinguni, sio kama vile mababa walivyo kula wakafa. Yeye
aulaye mkate huu ataishi milele. 59 Yesu aliyasema mambo haya ndani ya sinagogi
alipokuwa akifundisha huko Kapernaumu. 60 Ndipo wengi wa wanafunzi wake
waliposikia haya, wakasema, “Hili nifundisho gumu ni nani awezaye kulipokea?”
61 Yesu kwa sababu alijua ya kuwa wanafunzi wake walikuwa wakilinung'unikia

jambo hili, akawambia je jambo hili linawakwaza? [62] Basi itakuaje mtakapomwona
mwana wa Adamu akishuka kutoka alikokuwa kabla? [63] Ni Roho ndiye atoaye uzima.
Mwili haufaidii kitu chochote. Maneno niliyoyasema kwenu ni roho na ni uzima.
[64] Bado kuna watu kati yenu wasioamini." kwa sababu Yesu alijua tangu mwanzo
yule ambaye asiyeweza kuamini na yeye ambaye angemsaliti. [65] Akawambia, ni
kwa sababu hii niliwambia kwamba hakuna mtu awezaye kuja kwangu isipokuwa
amepewa na Baba." [66] Baada ya haya wanafunzi wake wengi walirudi nyuma na
hawakuambatana naye tena. [67] Yesu akawambia wale kumi na wawili, "Je na ninyi
mnataka kuondoka?" [68] Simoni Petro akamjibu, "Bwana twende kwa nani kwani
wewe unayo maneno ya uzima wa milele, [69] na tumeamini na kujua kuwa wewe ni
Mtakatifu wa Mungu." [70] Yesu akawambia, "Je mimi sikuwachagua ninyi, na mmoja
wenu ni ibilisi? [71] Sasa alikuwa akiongea kuhusu Yuda, mwana wa Simoni Iskariote,
kwa kuwa alikuwa ni yeye akiwa mmoja wa wale kumi na wawili, ambaye ndiye
angemsaliti Yesu.

# 7

[1] Na baada ya mambo haya Yesu alisafiri hivi katika Galilaya, kwa sababu
hakupenda kwenda Uyahudi kwa sababu wayahudi walikuwa wakifanya mipango ya
kumwua. [2] Sasa sikukuu ya Wayahudi, sikukuu ya Vibanda, ilikuwa karibu. [3] Ndipo
ndugu zake walipomwambia, "Ondoka mahali hapa uende Uyahudi, ili kwamba
wanafunzi wako vile vile wayaone matendo ufanyayo. [4] Hakuna afanyaye lolote kwa
siri iwapo yeye mwenyewe anataka kujulikana wazi. Iwapo unafanya mambo haya,
jionyeshe mwenyewe kwa ulimwengu." [5] Hata ndugu zake pia hawakumwamini.
[6] Ndipo Yesu alipowaambia, "Wakati wangu haujafika bado, lakini wakati wenu kila
mara uko tayari. [7] Ulimwengu hauwezi kuwachukia ninyi, bali unanichukia mimi
kwa sababu ninaushuhudia kuwa matendo yake ni maovu. [8] Pandeni kwenda katika
sikukuu; mimi siendi katika sikukuu hii kwa sababu muda wangu haujakamilika
bado." [9] Baada ya kusema mambo hayo kwao, alibaki Galilaya. [10] Hata hivyo,
ndugu zake walipokuwa wamekwenda katika sikukuu, ndipo naye alienda, siyo
kwa wazi bali kwa siri. [11] Wayahudi walikuwa wakimtafuta katika sikukuu na
kusema, "Yuko wapi?" [12] Kulikuwa na majadiliano mengi miongoni mwa makutano
juu yake. Wengine walisema, "Ni mtu mwema." Wengine walisema, "Hapana,
huwapotosha makutano." [13] Hata hivyo hakuna aliyezungumza wazi juu yake
kwa kuwaogopa Wayahudi. [14] Wakati sikukuu ilipofika katikati, Yesu alipanda
kwenda Hekaluni na kuanza kufundisha. [15] Wayahudi walikuwa wakishangaa na
kusema, "Kwa jinsi gani mtu huyu anajua mambo mengi? Hajasoma kamwe."
[16] Yesu akawajibu na kuwaambia, "Mafundisho yangu siyo yangu, bali ni yake
yeye aliyenituma. [17] Iwapo yeyote atapenda kufanya mapenzi yake yeye, atajua
kuhusu mafundisho haya, kama yanatoka kwa Mungu, au kama ninazungumza
kutoka kwangu mwenyewe. [18] Kila anayezungumza yatokayo kwake mwenywe
hutafuta utukufu wake, bali kila atafutaye utukufu wake yeye aliyemtuma, mtu
huyo ni wa kweli, na ndani yake hakuna kutotenda haki. [19] Musa hakuwapa
nyinyi sheria? Lakini hakuna hata mmoja kati yenu atendaye sheria. Kwa nini
mnataka kuniua? [20] Makutano wakajibu, "Una pepo. Nani anataka kukuua?"
[21] Yesu akajibu na akawaambia, "Nimetenda kazi moja, nanyi nyote mmeshangazwa
kwa sababu yake. [22] Musa aliwapa tohara (siyo kwamba inatoka kwa Musa,
bali ile inatoka kwa mababa), na katika Sabato mnamtahili mtu. [23] Iwapo mtu
atapokea tohara katika siku ya Sabato ili kwamba sheria ya Musa isivunjwe, kwa
nini mnanikasirikia mimi kwa sababu nimemfanya mtu kuwa mzima kabisa katika
Sabato? [24] Msihukumu kulingana na mwonekano, bali hukumuni kwa haki. [25] Baadhi

yao kutoka Yerusalemu wakasema, “Siye huyu wanayemtafuta kumwua? 26 Na
tazama, anaongea wazi wazi, na hawasemi chochote juu yake. Haiwezi ikawa
kwamba viongozi wanajua kweli kuwa huyu ni Kristo, inaweza kuwa? 27 Tunajua
huyu mtu anatokea wapi. Kristo atakapokuja, hata hivyo, hakuna atakayejua wapi
anakotoka.” 28 Yesu alikuwa akipaza sauti yake hekaluni, akifundisha na kusema,
“Ninyi nyote mnanijua mimi na mnajua nitokako. Sikuja kwa nafsi yangu, bali
yeye aliyenituma ni wa kweli, na hamumjui yeye. 29 Ninamjua yeye kwa sababu
nimetoka kwake na alinituma.” 30 Walikuwa wanajaribu kumkamata, lakini hakuna
hata mmoja aliyeinua mkono wake juu yake kwa sababu saa yake ilikuwa bado
haijafika. 31 Hata hivyo, wengi katika makutano walimwamini. Walisema, “Kristo
atakapokuja, atafanya ishara nyingi kuliko alizofanya mtu huyu?” 32 Mafarisayo
waliwasikia makutano wakinong'onezana mambo haya kuhusu Yesu, na wakuu
wa makuhani na Mafarisayo wakatuma maafisa ili kumkamata. 33 Ndipo Yesu
aliposema, “Bado kuna muda kitambo niko pamoja nanyi, na baadaye nitakwenda
kwake yeye aliyenituma. 34 Mtanitafuta wala hamtaniona; kule niendako, hamtaweza
kuja.” 35 Kwa hiyo Wayahudi wakasemezana wao kwa wao, “Mtu huyu atakwenda
wapi kwamba tusiweze kumuona? Ataenda kwa Waliotawanyika kati ya Wayunani
na kuwafundisha Wayunani? 36 Ni neno gani hili alilolisema, 'Mtanitafuta wala
hamtaniona; kule niendako hamtamweza kuja'?” 37 Sasa katika siku ya mwisho, siku
kubwa ya sikukuu, Yesu alisimama akapaza sauti, akisema, “Ikiwa yeyote ana kiu, na
aje kwangu anywe. 38 Yeye aniaminiye mimi, kama maandiko yalivyosema, kutoka
ndani yake itatiririka mito ya maji ya uzima.” 39 Lakini aliyasema haya kuhusu Roho,
ambaye wao wamwaminio watampokea; Roho alikuwa bado hajatolewa kwa sababu
Yesu alikuwa hajatukuzwa bado. 40 Baadhi ya makutano, waliposikia maneno haya,
walisema, “Kweli huyu ni nabii.” 41 Wengine walisema, “Huyu ni Kristo.” Lakini
wengine walisema, “nini, Kristo aweza kutoka Galilaya? 42 Maandiko hayajasema
kuwa Kristo atatokea katika ukoo wa Daudi na kutoka Bethlehemu, kijiji ambacho
Daudi alikuwa? 43 Hivyo, pale ukainuka mgawanyiko katikati ya makutano kwa ajili
yake. 44 Wengine kati yao wangelimkamata, lakini hakuna aliyenyoosha mikono yake
juu yake. 45 Ndipo wale maofisa wakarudi kwa wakuu wa makuhani na Mafarisayo,
nao wakawaambia, “Kwa nini hamjamleta?” 46 Maofisa wakajibu, “Hakuna mtu
aliyewahi kuzungumza kama huyu kabla.” 47 Ndipo Mafarisayo walipowajibu, “Na
nyinyi pia mmepotoshwa? 48 Kuna yeyote kati ya watawala anayemwamini, au
yeyote wa Mafarisayo? 49 Bali hawa makutano wasiojua sheria - wamelaaniwa.”
50 Nikodemo akawaambia (yeye aliyemwendea Yesu zamani, akiwa mmoja wa
Mafarisayo), 51 “Je sheria yetu inamhukumu mtu isipokuwa amesikilizwa kwanza na
kujua anachokifanya?” 52 Walijibu na kumwambia, “Na wewe pia unatokea Galilaya?
Tafuta na uone kwamba hakuna nabii aliyetokea Galilaya.” 53 (Zingatia: Baadhi ya
maneno ya Yohana 7: 53 - 8: 11 hayamo katika nakala bora za kale). Kisha kila mtu
alienda nyumbani kwake.

# 8

1 (Zingatia: Angalia ufafanuzi wa Yohana 7: 53 - 8: 11 hapo juu). Yesu alienda mlima
wa Mizeituni. 2 Mapema asubuhi akaja tena hekaluni, na watu wote wakamwendea;
akakaa na kuwafundisha. 3 Waandishi na Mafarisayo wakamletea mwanamke
aliyekamatwa katika kitendo cha kuzini. Wakamweka katikati. 4 (Zingatia: Angalia
ufafanuzi wa Yohana 7: 53 - 8: 11 hapo juu). Ndipo wakamwambia Yesu, “Mwalimu,
mwanamke huyu amekamatwa katika uzinzi, katika kitendo kabisa. 5 Sasa, katika
sheria, Musa ametuamuru kuwaponda mawe watu kama hawa, unasemaje juu yake?
6 Walisema haya ili kumtega ili kwamba wapate jambo la kumshitaki, lakini Yesu

akainama chini akaandika katika ardhi kwa kidole chake. 7 (Zingatia: Angalia
ufafanuzi wa Yohana 7: 53 - 8: 11 hapo juu). Walipoendelea kumwuliza, alisimama
na kuwaambia, “Yeye asiyekuwa na dhambi miongoni mwenu, awe wa kwanza
kumponda mawe.” 8 Akainama tena chini, akaandika katika ardhi kwa kidole chake.
9 (Zingatia: Angalia ufafanuzi wa Yohana 7: 53 - 8: 11 hapo juu). Waliposikia
hayo, waliondoka mmoja baada ya mwingine, kuanzia aliye mzee. Mwishowe
Yesu aliachwa peke yake, pamoja na mwanamke aliyekuwa katikati yao. 10 Yesu
alisimama na kumwambia, “Mwanamke, waliokushitaki wako wapi? Hakuna hata
mmoja aliyekuhukumu?” 11 Akasema, “Hakuna hata mmoja Bwana.” Yesu akasema,
“Hata mimi sikuhukumu. Nenda njia yako; kuanzia sasa na kuendelea usitende
dhambi tena.” 12 Tena Yesu akazungumza na watu akisema, “Mimi ni nuru ya
ulimwengu; yeye anifuataye hatatembea gizani bali atakuwa na nuru ya uzima.”
13 Mafarisayo wakamwambia, “Unajishuhudia mwenyewe; ushuhuda wako siyo
wa kweli.” 14 Yesu alijibu akawaambia, “Hata kama nitajishuhudia mwenyewe,
ushuhuda wangu ni kweli. Ninajua mahali nilikotoka na kule ninakoenda, lakini
ninyi hamjui mahali ninapotoka au kule ninakoenda. 15 Nyinyi mnahukumu kimwili;
mimi simhukumu yeyote. 16 Mimi hata nikihukumu, hukumu yangu ni kweli kwa
sababu siko peke yangu, bali niko pamoja na baba aliyenituma. 17 Ndiyo, na katika
sheria yenu imeandikwa kwamba ushuhuda wa watu wawili ni kweli. 18 Mimi
ndiye ninayejishuhudia, na Baba aliyenituma ananishuhudia.” 19 Wakamwambia,
“Baba yako yuko wapi?” Yesu akajibu, “mimi hamnijui wala Baba yangu hammjui;
mngelikuwa mnanijua mimi, mngemjua na Baba yangu pia.” 20 Alisema maneno haya
akiwa karibu na hazina alipokuwa akifundisha hekaluni, na hakuna hata mmoja
aliyemkamata kwa sababu saa yake ilikuwa bado haijafika. 21 Basi akawaambia
tena, “Ninaenda zangu; mtanitafuta na mtakufa katika dhambi zenu. Kule niendako,
hamuwezi kuja.” 22 Wayahudi wakasema, “Atajiua mwenyewe, yeye ambaye alisema,
'kule niendako hamuwezi kuja'?” 23 Yesu akawaambia, “Mnatoka chini; mimi natoka
juu. Ninyi ni wa Ulimwengu huu; mimi si wa ulimwengu huu. 24 Kwa hiyo,
naliwaambieni kuwa mtakufa katika dhambi zenu. Vinginevyo muamini kuwa MIMI
NDIYE, mtakufa katika dhambi zenu”. 25 Kwa hiyo wakamwambia, “Wewe ni nani?”
Yesu akawaambia, Yale niliyowaambia tangu mwanzo. 26 Ninayo mambo mengi ya
kuzungumza na kuhukumu juu yenu. Hata hivyo, yeye aliyenituma ni wa kweli;
na mambo niliyoyasikia kutoka kwake, mambo haya nayasema kwa Ulimwengu.”
27 Hawakumuelewa kwamba alikuwa akiongea nao kuhusu Baba. 28 Yesu akasema,
“Mtakapomwinua juu Mwana wa Mtu, ndipo mtakapojua kuwa MIMI NDIYE, na
kwamba sifanyi lolote kwa nafsi yangu. Kama Baba alivyonifundisha, ninazungumza
mambo haya. 29 Yeye aliyenituma yuko pamoja nami, na yeye hajaniacha peke yangu,
kwani kila mara nafanya yale yanayompendeza.” 30 Wakati Yesu akisema mambo
haya, wengi walimwamini. 31 Yesu akasema kwa wale Wayahudi waliomwamini,
“Ikiwa mtakaa katika neno langu, ndipo mtakuwa wanafunzi wangu kweli, 32 nanyi
mtaijua kweli, na kweli itawaweka huru.” 33 Walimjibu, “Sisi ni uzao wa Ibrahimu
na kamwe hatujawahi kwa chini ya utumwa wa yeyote; utasemaje, “Tutawekwa
huru?” 34 Yesu aliwajibu, “Amini, amini, nawaambia, kila atendaye dhambi ni
mtumwa wa dhambi. 35 Mtumwa hakai nyumbani wakati wote; mwana hudumu
siku zote. 36 Kwa hiyo, ikiwa Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kabisa.”
37 Ninajua kwamba ninyi ni uzao wa Ibrahimu; mnatafuta kuniua kwa sababu
neno langu halina nafasi ndani yenu. 38 Ninasema mambo ambayo nimeyaona
pamoja na Baba yangu, na ninyi vile vile mnafanya mambo ambayo mliyasikia
kutoka kwa baba yenu.” 39 Walijibu na kumwambia, “Baba yetu ni Abrahamu.”
Yesu akawaambia, Kama mngelikuwa watoto wa Ibrahimu, mngefanya kazi za

Ibrahimu. 40 Hata sasa mnatafuta kuniua, mtu aliyewaambia ukweli kwamba
nilisikia kutoka kwa Mungu. Abrahamu hakufanya hivi. 41 Mnafanya kazi za
baba yenu." Wakamwambia, "Hatukuzaliwa katika uzinzi, tunaye Baba mmoja,
Mungu." 42 Yesu akawaambia, "Ikiwa Mungu ni Baba yenu, mngenipenda mimi,
kwa maana nimetoka kwa Mungu; wala sikuja kwa nafsi yangu, bali yeye alinituma.
43 Kwa nini hamyaelewi maneno yangu? Kwa sababu hamuwezi kuvumilia kuyasikia
maneno yangu. 44 Ninyi ni wa baba yenu, shetani, na mnataka kuzitenda tamaa
za baba yenu. Alikuwa mwuaji tangu mwanzo na hawezi kusimama katika kweli
kwa sababu kweli haimo ndani yake. Anapoongea uongo, anaongea kutoka kwenye
asili yake kwa sababu ni mwongo na baba wa uongo. 45 Hata sasa, kwa sababu
ninasema iliyo kweli, hamniamini. 46 Ni nani kati yenu anayenishuhudia kuwa nina
dhambi? ikiwa ninasema iliyo kweli, kwa nini hamniamini? 47 Yeye aliye wa Mungu
huyasikia maneno ya Mungu; ninyi hamyasikii kwa sababu ninyi si wa Mungu."
48 Wayahudi wakamjibu na kumwambia, hatujasema kweli kuwa wewe ni Msamaria
na una pepo?" 49 Yesu akajibu, sina pepo; lakini namheshimu Baba yangu, nanyi
hamniheshimu. 50 Sitafuti utukufu wangu; kuna mmoja atafutaye na kuhukumu.
51 Amini, amini, nawaambia, iwapo yeyote atalishika neno langu, hataona mauti
kamwe." 52 Wayahudi wakamwambia, "Sasa tumejua kuwa una pepo. Abrahamu na
mabii walikufa; lakini unasema, 'Ikiwa mtu atalishika neno langu, hataonja mauti'.
53 Wewe si mkuu kuliko baba yetu Abrahamu aliyekufa, sivyo? Manabii pia walikufa.
Wewe wajifanya kuwa nani?" 54 Yesu akajibu, "Ikiwa nitajitukuza mwenyewe,
utukufu wangu ni bure; ni Baba yangu anayenitukuza - yule mnayemsema kuwa ni
Mungu wenu. 55 Ninyi hamjamjua yeye, lakini mimi namjua yeye. Ikiwa nitasema,
'simjui,' nitakuwa kama nyinyi, muongo. Hata hivyo, ninamjua na maneno yake
nimeyashika. 56 Baba yenu Abrahamu alishangilia atakavyoiona siku yangu; aliiona
na alifurahi." 57 Wayahudi wakamwambia,"Haujafikisha umri wa miaka hamsini
bado, nawe umemuona Ibrahimu?" 58 Yesu akawaambia, "Amini, amini, nawaambia,
kabla Abrahamu hajazaliwa, MIMI NIKO." 59 Ndipo waliokota mawe wapate kumpiga,
lakini Yesu alijificha na akatoka nje ya hekalu.

# 9

1 Wakati, kama Yesu alipokuwa akipita, alimwona mtu kipofu tangu kuzaliwa
kwake. 2 Wanafunzi wake wakamwuliza, "Rabi, nani aliyetenda dhambi, mtu huyu
au wazazi wake, hata azaliwe kipofu?" 3 Yesu akawajibu, "Siyo huyu mtu wala
wazazi wake waliotenda dhambi, bali kazi za Mungu zipate kufunuliwa kupitia
kwake. 4 Tunapaswa kufanya kazi zake yeye aliyenituma wakati bado ni mchana.
Usiku waja wakati ambapo hakuna atakayeweza kufanya kazi. 5 Wakati niwapo
ulimwenguni, mimi ni nuru ya ulimwengu." 6 Baada ya Yesu kusema maneno haya,
alitema kwenye ardhi, alifanya tope kwa mate, na akampaka yule mtu machoni na
lile tope. 7 Akamwambia, nenda kaoge katika kisima cha Siloam (Inayotafsiriwa kama
'aliyetumwa')." Kwa hiyo huyo mtu alienda, akanawa, na akarudi, anaona. 8 Majirani
wa yule mtu na wale waliomuona mwanzo kama mwombaji walisema, Je! huyu siye
yule mtu aliyekuwa akikaa na kuomba?" wengine walisema, "Ni yeye." 9 Na wengine
walisema, "Hapana, bali anafanana naye." Lakini alikuwa akisema, "Ni mimi."
10 Wakamwambia, "Sasa macho yako yalifunguliwaje?" 11 Alijibu, mtu aitwaye Yesu
alifanya tope na kupaka macho yangu na kuniambia, 'Nenda Siloam ukanawe.'
Kwa hiyo nilienda, na nikanawa, na nikapata kuona tena." 12 Wakamwambia,
"Yuko wapi?" Alijibu, "Sijui." 13 Wakampeleka yule mtu aliyewahi kuwa kipofu
kwa Mafarisayo. 14 Nayo ilikuwa siku ya Sabato wakati Yesu alipotengeneza tope
na kuyafumbua macho yake. 15 Ndipo tena Mafarisayo wakamwuliza alipataje

kuona. Aliwaambia, “Aliweka tope katika macho yangu, nikanawa, na sasa naweza
kuona.” 16 Baadhi ya Mafarisayo wakasema, “Mtu huyu hajatoka kwa Mungu
kwa sababu haishiki Sabato.” Wengine walisema, “Inawezekanaje mtu mwenye
dhambi kufanya ishara kama hizo?” Kwa hiyo kukawa na mgawanyiko kati
yao. 17 Ndipo walipomwuliza yule kipofu tena, “Unasemaje juu yake kwa sababu
aliyafungua macho yako?” Kipofu akasema, “Ni nabii.” 18 Hata wakati huu Wayahudi
hawakumwamini kwamba alikuwa kipofu naye amepata kuona mpaka walipowaita
wazazi wake yeye aliyepata kuona. 19 Waliwauliza wazazi, Je, huyu ni mtoto
wenu mnayesema alizaliwa kipofu? amewezaje sasa kuona?” 20 Hivyo wazazi
wake wakamjibu, “Tunajua kuwa huyu ni mtoto wetu na kwamba alizaliwa kipofu.
21 Jinsi gani sasa anaona, hatujui, na yeye aliyemfumbua macho yake, hatumjui.
Mwulizeni yeye. Ni mtu mzima. Anaweza kujieleza mwenyewe.” 22 Wazazi wake
walisema mambo haya, kwa sababu waliwaogopa Wayahudi. Kwa vile Wayahudi
walikuwa wamekubaliana tayari kuwa, ikiwa yeyote atakiri kuwa Yesu ni Kristo,
atatengwa na Sinagogi. 23 Kwa sababu hii, wazazi wake walisema, “Ni mtu mzima,
mwulizeni yeye.” 24 Kwa hiyo kwa mara ya pili, walimwita yule mtu aliyewahi
kuwa kipofu na kumwambia, “Mpe Mungu utukufu. Tunajua kwamba mtu huyu
ni mwenye dhambi.” 25 Ndipo yule mtu alijibu, “Awe ni mwenye dhambi, mimi
sijui. Kitu kimoja ninachokijua: nilikuwa kipofu, na sasa ninaona.” 26 Ndipo
walipomwambia, “Amekufanyia nini? Aliyafumbuaje macho yako?” 27 Alijibu,
“Nimekwishawaambia tayari, na nyinyi hamkusikiliza! Kwa nini mnataka kusikia
tena? Nanyi hamtaki kuwa wanafunzi wake pia, sivyo? 28 Walimtukana na kusema,
“Wewe ni mwanafunzi wake, lakini sisi ni wanafunzi wa Musa. 29 Tunajua kwamba
Mungu alizungumza na Musa, lakini kwa huyu mtu, hatujui kule atokako.” 30 Yule
mtu akajibu na kuwaambia, “Kwa nini, hili ni jambo la kushangaza, kwamba
hamjui anakotoka, na bado ameyafumbua macho yangu. 31 Tunajua kuwa Mungu
hawasikilizi wenye dhambi, lakini ikiwa mtu yeyote anamwabudu Mungu na hufanya
mapenzi yake, Mungu humsikiliza. 32 Tangu kuanza kwa Ulimwengu haijawahi
kamwe kusikiwa kwamba yeyote ameyafumbua macho ya mtu aliyezaliwa kipofu.
33 Ikiwa mtu huyu hakutoka kwa Mungu, asingelifanya chochote.” 34 Walijibu na
kumwambia, “Ulizaliwa katika dhambi kabisa, na wewe unatufundisha sisi?” Ndipo
walipomfukuza kutoka katika sinagogi. 35 Yesu alisikia kwamba wamemwondoa
kwenye sinagogi. Alimpata na kumwambia, “Unamwamini Mwana wa Mtu?”
36 Alijibu na kusema, “Ni nani, Bwana, ili nami nipate kumwamini?” 37 Yesu
akamwambia, “Umeshamuona, naye unayezungumza naye ndiye.” 38 Yule mtu
akasema, “Bwana, Naamini.” Ndipo akamsujudia. 39 Yesu akasema, “Kwa hukumu
nimekuja katika Ulimwengu huu ili kwamba wale wasioona wapate kuona na wale
wanaoona wawe vipofu.” 40 Baadhi ya Mafarisayo waliokuwa pamoja naye wakasikia
maneno hayo na kumwuliza, “Na sisi pia ni vipofu?” 41 Yesu akawaambia, “Kama
mngelikuwa vipofu, msingelikuwa na dhambi. Hata hivyo, sasa mnasema, 'Tunaona,'
dhambi yenu inakaa.”

# 10

1 Amin, Amini nawaambieni, yule asiyeingia kwa kupitia mlango wa zizi la
kondoo, lakini anapanda kwa njia nyingine, mtu huyo ni mwizi na mnyang'anyi.
2 Yeye aingiaye mlangoni ni mchungaji wa kondoo. 3 Kwake mlinzi wa mlango
humfungulia. Kondoo waisikia sauti yake na huwaita kondoo zake kwa majina yao
na kuwatoa nje. 4 Atakapowatoa nje hao walio wake, huwatangulia, na kondoo
humfuata, kwa sababu wanaijua sauti yake. 5 Hawatamfuata mgeni lakini badala
yake watamuepuka, kwa sababu hawazijui sauti za wageni.” 6 Yesu alisema mfano

huu kwao, lakini hawakuyaelewa mambo haya ambayo alikuwa akisema kwao.
7 Yesu akasema nao tena, “Amini, amini, nawaambia, Mimi ni mlango wa kondoo.
8 Wote walionitangulia ni wezi na wanyang'anyi, lakini kondoo hawakuwasikiliza.
9 Mimi ni mlango. Yeyote aingiaye kupitia kwangu, ataokolewa; ataingia ndani na
kutoka, naye atajipatia malisho. 10 Mwizi haji isipokuwa kuiba, kuua, na kuangamiza.
Nimekuja ili kwamba wapate uzima na wawe nao tele. 11 Mimi ni mchungaji
mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo. 12 Mtumishi
aliyeajiriwa, na siyo mchungaji, ambaye kondoo si mali yake, huwaona mbwa mwitu
wakija na huwaacha na kuwakimbia kondoo. 13 Na mbwa mwitu huwakamata
na kuwatawanya. Hukimbia kwa sababu ni mtumishi wa kuajiriwa na hawajali
kondoo. 14 Mimi ni mchungaji mwema, na ninawajua walio wangu, nao walio
wangu wananijua mimi. 15 Baba ananijua, nami namjua Baba, nami nautoa uhai
wangu kwa ajili ya kondoo. 16 Ninao kondoo wengine ambao si wa zizi hili. Hao
pia, yanipasa kuwaleta, nao wataisikia sauti yangu ili kwamba pawepo na kundi
moja na mchungaji mmoja. 17 Hii ndiyo sababu Baba ananipenda: Niutoe uhai
wangu halafu niutwae tena. 18 Hakuna auchukuaye kutoka kwangu, lakini mimi
nautoa mwenyewe. Ninayo mamlaka ya kuutoa, na ninayo mamlaka ya kuutwaa
pia. Nimelipokea agizo hili kutoka kwa Baba.” 19 Mgawanyiko tena ukatokea kati
ya wayahudi kwa sababu ya maneno haya. 20 Wengi wao wakasema, “Ana pepo na
ni kichaa. Kwa nini mnamsikiliza?” 21 Wengine wakasema, “Haya siyo maneno ya
mtu aliyepagawa na mapepo. Pepo linaweza kufungua macho ya kipofu?” 22 Ndipo
ikaja Sikukuu ya Kuwekwa Wakfu Yerusalemu. 23 Ulikuwa wakati wa baridi, na
Yesu alikuwa akitembea hekaluni katika ukumbi wa Selemani. 24 Ndipo Wayahudi
walipomzunguka na kumwambia, “Mpaka lini utatuweka katika mashaka? kama
wewe ni Kristo, tuambie wazi. 25 Yesu akawajibu, “Nimekwisha waambia lakini
hamuamini. Kazi nizifanyazo kwa jina la Baba yangu, hizo zinashuhudia juu yangu.
26 Hata hivyo hamuamini kwa sababu ninyi si kondoo wangu. 27 Kondoo wangu
waisikia sauti yangu; Nawajua, nao wanifuata mimi. 28 Nimewapa uzima wa milele;
hawataangamia kamwe, na hakuna hata mmoja atakayewanyakuwa kutoka mkononi
mwangu. 29 Baba yangu, aliyenipa hao, ni mkuu kuliko wengine wote, na hakuna
hata mmoja aliye na uwezo wa kuwanyakua kutoka mkononi mwa Baba. 30 Mimi
na Baba tu mmoja.” 31 Wakabeba mawe ili wamponde tena. 32 Yesu akawajibu,
“Nimeshawaonesha kazi nyingi nzuri kutoka kwa Baba. Kwa kazi zipi kati ya hizo
mnataka kuniponda mawe?” 33 Wayahudi wakamjibu, “Hatukupondi mawe kwa kazi
yoyote iliyo nzuri, lakini kwa kukufuru, kwa sababu wewe, uliye mtu, unajifanya
kuwa Mungu.” 34 Yesu akawajibu, “Haikuandikwa katika sheria yenu, 'Nilisema,
“Ninyi ni miungu”'?” 35 Ikiwa aliwaita miungu, kwa wale ambao Neno la Mungu
liliwajilia (na Maandiko hayawezi kuvunjwa), 36 mnasema juu ya yule ambaye Baba
alimtoa na kumtuma katika ulimwengu, 'Unakufuru,' kwa sababu nilisema, 'mimi
ni Mwana wa Mungu'? 37 “Ikiwa sifanyi kazi za Baba yangu, msiniamini. 38 Hata
hivyo, ikiwa ninazifanya, hata kama hamniamini, ziaminini kazi ili kwamba muweze
kujua na kufahamu kwamba Baba yuko ndani yangu na mimi niko ndani ya Baba.”
39 Wakajaribu tena kumkamata Yesu, lakini alienda zake kutoka mikononi mwao.
40 Yesu akaenda zake tena ng'ambo ya Yordani sehemu ambayo Yohana alikuwa
akibatiza kwanza, na akakaa huko. 41 Watu wengi wakaja kwa Yesu. Waliendelea
kusema, “Yohana kweli hakufanya ishara yoyote, lakini mambo yote aliyoyasema
Yohana juu ya huyu mtu ni ya kweli.” 42 Watu wengi wakamwamini Yesu hapo.

## 11

1 Basi mtu mmoja jina lake Lazaro alikuwa mgonjwa. Alitokea Bethania, kijiji

cha Mariamu na dada yake Martha. 2 Alikuwa ni Mariamu yule yule aliyempaka
Bwana Marhamu na kumfuta miguu yake kwa nywele zake, ambaye ndugu yake
Lazaro alikuwa ni mgonjwa. 3 Ndipo dada hawa walituma ujumbe kwa Yesu na
kusema, “Bwana, angalia yule umpendaye anaumwa.” 4 Yesu aliposikia alisema,
“Ugonjwa huu si wa mauti, lakini, badala yake ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu
ili kwamba Mwana wa Mungu apate kutukuzwa katika huo Ugonjwa.” 5 Yesu
alimpenda Martha na dada yake na Lazaro. 6 Aliposikia kuwa Lazaro ni mgonjwa,
Yesu alikaa siku mbili zaidi mahali alipokuwa. 7 Ndipo baada ya hili aliwaambia
wanafunzi wake, “Twendeni Uyahudi tena.” 8 Wanafunzi wakamwambia, “Rabi,
Wayahudi walikuwa wakijaribu kukuponda mawe, na wewe unataka kurudi huko
tena?” 9 Yesu akawajibu, “Saa za mchana si kumi na mbili? Mtu anapotembea
mchana hawezi kujikwaa, kwa sababu anaona kwa nuru ya mchana. 10 Hata
hivyo, ikiwa atatembea usiku, atajikwaa kwa sababu nuru haiko ndani yake.”
11 Yesu akasema mambo haya, na baada ya mambo haya, akawaambia, “Rafiki
yetu Lazaro amelala, lakini ninakwenda ili kwamba nipate kumuamsha kutoka
usingizini.” 12 Ndipo wanafunzi wakamwambia, “Bwana, kama amelala, ataamka.
13 Wakati huu Yesu alikuwa akizungumza habari za kifo cha Lazaro, lakini wao
walidhani anazungumza juu ya kulala usingizi. 14 Ndipo Yesu akazungumza nao
wazi wazi, “Lazaro amekufa. 15 Nina furaha kwa ajili yenu, kwamba sikuwepo
kule ili kwamba mpate kuamini. Twendeni kwake.” 16 Basi Tomaso, aliyeitwa
Pacha, aliwaambia wanafunzi wenzake, “Nasi twendeni pia tukafe pamoja na Yesu.”
17 Wakati Yesu alipokuja, alikuta kwamba Lazaro tayari amekwishakuwa kaburini
siku nne. 18 Nayo Bethania ilikuwa karibu na Yerusalemu kama kilomita arobaini na
tano hivi. 19 Wengi kati ya Wayahudi wakaja kwa Martha na Mariamu kuwafariji
kwa ajili ya ndugu yao. 20 Ndipo Martha aliposikia kuwa Yesu anakuja, aliienda
kukutana naye, lakini Mariamu aliendelea kukaa nyumbani. 21 Ndipo Martha
akamwambia Yesu, “Bwana, kama ungelikuwa hapa, kaka yangu asingelikufa. 22 Hata
sasa, najua ya kuwa lolote utakaloomba kutoka kwa Mungu, atakupatia.” 23 Yesu
akamwambia, kaka yako atafufuka tena.” 24 Martha akamwambia, najua kwamba
atafufuka katika ufufuo siku ya mwisho.” 25 Yesu akamwambia, “Mimi ni ufufuo na
uzima; yeye aniaminiye, ingawa atakufa, hata hivyo atakuwa anaishi; 26 na yeye
aishiye na kuniamini mimi hatakufa. Unaamini hili?” 27 Akamwambia, “Ndiyo,
Bwana naamini kwamba wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu, yeye ajaye katika
ulimwengu.” 28 Alipokwisha kusema hili, alienda zake na kumwita dada yake
Mariamu faraghani. Akasema, “Mwalimu yuko hapa na anakuita.” 29 Mariamu
aliposikia haya, aliinuka kwa haraka na kwenda kwa Yesu. 30 Naye Yesu alikuwa
hajaja bado ndani ya kijiji, bali alikuwa bado mahali alipokutana na Martha.
31 Ndipo Wayahudi waliokuwa na Mariamu katika nyumba na wale waliokuwa
wakimfariji, walipomuona akiinuka haraka na kutoka nje, walimfuata; walidhani
kuwa anaenda kaburini ili akalie huko. 32 Ndipo Mariamu, alipofika pale Yesu
alipokuwa alimuona na, alianguka chini ya miguu yake na kumwambia, “Bwana,
kama ungelikuwa hapa, ndugu yangu asingelikufa.” 33 Yesu alipomuona analia,
na Wayahudi waliokuja pamoja naye walikuwa wakilia pia, aliomboleza katika
roho na kufadhaika; 34 akasema, “Mmemlaza wapi? wakamwambia, Bwana, njoo
utazame.” 35 Yesu akalia. 36 Ndipo Wayahudi wakasema, “Angalia alivyompenda
Lazaro!” 37 Lakini wengine kati yao wakasema, “Siyo huyu, mtu aliyeyafumbua
macho ya yule aliyekuwa kipofu, hakuweza kumfanya huyu mtu asife?” 38 Ndipo
Yesu, hali akiomboleza nafsini mwake tena, alienda kwenye kaburi. Sasa lilikuwa
pango, na jiwe limewekwa juu yake. 39 Yesu akasema, “Liondoweni jiwe.” Martha,

dada yake na Lazaro, yeye aliyekufa, akamwambia Yesu, “Bwana, kwa muda huu,
mwili utakuwa umeoza, kwa sababu amekwishakuwa maiti kwa siku nne.” 40 Yesu
akamwambia, “Mimi sikukuwaambia ya kwamba, kama ukiamini, utauona utukufu
wa Mungu?” 41 Kwa hiyo wakaliondoa jiwe. Yesu akainua macho yake juu na kusema,
“Baba, nakushukuru kwa kuwa unanisikiliza. 42 Nilijua kwamba unanisikia mara
zote, lakini ni kwa sababu ya kusanyiko ambalo limesimama kunizunguka kwamba
nimesema haya, ili kwamba wapate kuamini kuwa wewe umenituma.” 43 Baada
ya kusema haya, alilia kwa sauti kubwa, “Lazaro, toka nje!” 44 Mfu alitoka nje
amefungwa mikono na miguu kwa sanda za kuzikia, na uso wake ulifungwa na
kitambaa.” Yesu akawaambia, “Mfungueni mkamwache aende.” 45 Ndipo Wayahudi
wengi waliokuja kwa Mariamu na kuona Yesu alichofanya, walimwamini; 46 lakini
baadhi yao walienda kwa Mafarisayo na kuwaambia mambo aliyoyafanya Yesu.
47 Ndipo wakuu wa Makuhani na Mafarisayo wakakusanyika pamoja katika baraza
na kusema, “Tutafanya nini? Mtu huyu anafanya ishara nyingi. 48 Ikiwa tutamwacha
hivi peke yake, wote watamwamini; Warumi watakuja na kuchukua vyote mahali
petu na taifa letu.” 49 Hata hivyo, mtu mmoja kati yao, Kayafa, aliyekuwa kuhani
Mkuu mwaka huo, akawaambia, “ Hamjui chochote kabisa. 50 Hamfikirii kwamba
yafaa kwa ajili yenu kwamba mtu mmoja yapasa kufa kwa ajili ya watu kuliko taifa
lote kuangamia.” 51 Haya hakuyasema kwa sababu yake mwenyewe, badala yake,
kwa kuwa alikuwa kuhani mkuu mwaka ule, alitabiri kwamba Yesu atakufa kwa ajili
ya taifa; 52 na si kwa taifa peke yake, bali Yesu apate vile vile kuwakusanya watoto wa
Mungu ambao wametawanyika sehemu mbali mbali. 53 Kwa hiyo kuanzia siku hiyo
na kuendelea wakapanga namna ya kumwua Yesu. 54 Yesu hakutembea tena wazi
wazi kati ya Wayahudi, bali aliondoka hapo na kwenda nchi iliyo karibu na jangwa
katika mji uitwao Efraimu. Hapo alikaa na wanafunzi. 55 Basi Pasaka ya Wayahudi
ilikuwa karibu, na wengi wakapanda kwenda Yerusalemu nje ya mji kabla ya Pasaka
ili wapate kujitakasa wenyewe. 56 Walikuwa wakimtafuta Yesu, na kuzungumza
kila mmoja walipokuwa wamesimama hekaluni, “Mnafikiri nini? Kwamba hatakuja
katika sikukuu?” 57 Wakati huu wakuu wa makuhani na Mafarisayo walikuwa
wametoa amri kwamba ikiwa mmoja atajua Yesu alipo, anapaswa kutoa taarifa ili
kwamba wapate kumkamata.

# 12

1 Siku sita kabla ya Pasaka, Yesu alienda Bethania, alipokuwapo Lazaro, yeye
ambaye alimfufua kutoka katika wafu. 2 Basi wakamwandalia chakula cha jioni
huko, na Martha akamtumikia, wakati huo Lazaro alikuwa mmoja wapo wa wale
walioketi chakulani pamoja na Yesu. 3 Kisha Mariamu akachukua ratli ya manukato
yaliyotengenezwa kwa nardo safi, yenye thamani kubwa, akampaka Yesu miguuni,
na kumfuta miguu kwa nywele zake; nyumba yote ilijaa harufu ya manukato.
4 Yuda Iskariote, mmoja wa wale wanafunzi wake, ambaye ndiye atakayemsaliti Yesu,
akasema, 5 “Kwanini manukato haya yasingeuzwa kwa dinari mia tatu na wakapewa
maskini?” 6 Naye aliyasema hayo, si kwa kuwahurumia maskini, bali kwa sababu
alikuwa mwizi: yeye ndiye aliyeshika mfuko wa fedha na alikuwa anachukua baadhi
ya vilivyowekwa humo kwa ajili yake mwenyewe. 7 Yesu alisema, “Mwache aweke
alicho nacho kwa ajili ya siku ya maziko yangu. 8 Maskini mtakuwa nao siku zote;
lakini hamtakuwa nami siku zote.” 9 Basi umati mkubwa wa Wayahudi walipata
kujua ya kuwa Yesu yuko huko, nao wakaja, si kwa ajili ya Yesu tu, ila wamwone
na Lazaro ambaye Yesu alimfufua kutoka katika wafu. 10 Nao wakuu wa makuhani
wakafanya shauri ili wamue Lazaro; 11 maana kwa ajili yake wengi katika Wayahudi
walienda zao na wakamwamini Yesu. 12 Na siku ya pili yake umati mkubwa walikuja

kwenye sikukuu. Waliposikia ya kuwa Yesu anakuja Yerusalemu, 13 walichukua
matawi ya miti ya mitende na kutoka nje kwenda kumlaki na wakapiga kelele,
“Hosana! Amebarikiwa yeye ajaye kwa jina la Bwana, Mfalme wa Israeli.” 14 Yesu
alimpata mwana-punda akampanda; kama vile ilivyoandikwa, 15 “Usiogope, binti
Sayuni; tazama, Mfalme wako anakuja, amepanda mwana-punda.” 16 Wanafunzi
wake hawakuyaelewa mambo haya hapo kwanza; lakini Yesu alipotukuzwa, ndipo
walipokumbuka ya kuwa mambo haya aliandikiwa yeye na ya kwamba wametenda
mambo haya kwake. 17 Basi lile kundi la watu waliokuwepo pamoja na Yesu wakati
alipomwita Lazaro kutoka kaburini, wakashuhudia kwa wengine. 18 Na ilikuwa kwa
sababu hii pia kwamba kundi la watu walikwenda kumlaki kwasababu walisikia
ya kwamba ameifanya ishara hiyo. 19 Mafarisayo wakasemezana wao kwa wao,
“Tazama, sasa hamwezi kufanya lolote; tazama, ulimwengu umekwenda kwake.”
20 Sasa baadhi ya Wayunani walikuwa miongoni mwa wale waliokuwa wakienda
kuabudu kwenye sikukuu. 21 Hawa walimwendea Filipo, ambaye alitoka Bethsaida
ya Galilaya, wakamwomba wakisema, “Bwana, sisi tunatamani kumwona Yesu.”
22 Filipo akaenda akamwambia Andrea; Andrea na Filipo wakaenda na kumwambia
Yesu. 23 Yesu akawajibu akasema, “Saa imefika kwa ajili ya Mwana wa Adamu
kutukuzwa. 24 Amini, amini, nawaambia, chembe ya ngano isipoanguka katika nchi
ikafa, hukaa hali iyo hiyo peke yake; bali ikifa, itazaa matunda mengi. 25 Yeye
apendaye uhai wake ataupoteza; bali yeye auchukiaye uhai wake katika ulimemngu
huu atausalimisha hata uzima wa milele. 26 Mtu yeyote akinitumikia mimi, na
anifuate; nami nilipo, ndipo na mtumishi wangu atakapokuwapo. Mtu yeyote
akinitumikia, Baba atamheshimu. 27 Sasa roho yangu imefadhaika: nami nisemeje?
'Baba, uniokoe katika saa hii'? Lakini ni kwa kusudi hii nimeifikia saa hii. 28 Baba,
ulitukuze jina lako.” Kisha sauti ikaja kutoka mbinguni na kusema, “Nimelitukuza
nami nitalitukuza tena.” 29 Basi mkutano uliosimama karibu naye wakasikia,
wakasema ya kwamba kumekuwa ngurumo. Wengine walisema, “Malaika amesema
naye.” 30 Yesu akajibu na kusema, “Sauti hii haikuja kwa ajili yangu, bali kwa ajili
yenu. 31 Sasa hukumu ya ulimwengu huu ipo: Sasa mkuu wa ulimwngu huu atatupwa
nje. 32 Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu.” 33 Aliyanena hayo
akionesha ni mauti gani atakayokufa. 34 Mkutano wakamjibu, “Sisi tumesikia katika
sheria ya kwamba Kristo atadumu hata milele. Nawe wasemaje, 'Mwana Adamu
lazima ainuliwe juu'? Huyu Mwana wa Mtu ni nani?” 35 Basi Yesu akawaambia,
“Nuru ingalipo pamoja nanyi muda kidogo. Enendeni maadamu mnayo nuru, ili
kwamba giza lisije likawaweza. Yeye aendaye gizani hajui aendako. 36 Mngali
mnayo nuru, iaminini nuru hiyo ili mpate kuwa wana wa nuru.” Yesu aliyasema
haya na kisha akaenda zake akajificha wasimwone. 37 Ingawa Yesu alifanya ishara
nyingi namna hiyo mbele yao, bado hawakumwamini 38 ili litimie neno la nabii
Isaya, alilosema: “Bwana, ni nani aliyezisadiki habari zetu? Na mkono wa Bwana
amefunuliwa nani?” 39 Ndio sababu wao hawakuamini, maana Isaya alisema tena,
40 “Amewapofusha macho, na ameifanya migumu mioyo yao; wasije wakaona kwa
macho yao na wakafahamu kwa mioyo yao, na wakaongoka nami nikawaponya.”
41 Isaya alisema maneno hayo kwa kuwa aliuona utukufu wa Yesu na akanena habari
zake. 42 Walakini, hata wakuu wengi walimwamini Yesu; lakini kwa sababu ya
Mafarisayo, hawakukiri ili wasije wakatengwa na sinagogi. 43 Walipenda sifa za
wanadamu kuliko sifa zitokazo kwa Mungu. 44 Yesu akapaza sauti na kusema, “Yeye
aniaminiye mimi, haniamini mimi tu bali na yeye aliyenituma mimi, 45 naye anionaye
mimi anamuona yeye aliyenituma. 46 Mimi nimekuja kama nuru ulimwenguni ili
kila mtu aniaminiye mimi asikae gizani. 47 Ikiwa mtu yeyote atayasikia maneno
yangu lakini asiyashike, mimi simhukumu; maana sikuja ili niuhukumu ulimwengu,

bali niuokoe ulimwengu. 48 Yeye anikataye mimi na asiyeyakubali maneno yangu,
anaye amhukumuye: neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho.
49 Maana mimi sikunena kwa nafsi yangu tu. Bali ni Baba aliyenipeleka, yeye
mwenyewe ameniagiza nitakayonena na nitakayosema. 50 Nami najua ya kuwa agizo
lake ni uzima wa milele; basi hayo ninenayo mimi - kama Baba alivyoniambia, ndivyo
ninenavyo kwao."

# 13

1 Sasa kabla ya sikukuu ya pasaka, kwa sababu Yesu alifahamu kuwa saa yake
imefika ambayo atatoka katika dunia hii kwenda kwa baba, akiwa amewapenda watu
wake ambao walikuwa duniani, aliwapenda upeo. 2 Na ibilisi alikuwa amewekwa
tayari katika moyo wa Yuda Isikariote, mwana wa simoni, kumsaliti Yesu. 3 Yesu
alifahamu kuwa baba ameweka vitu vyote katika mikono yake na kwamba ametoka
kwa Mungu na alikuwa anakwenda tena kwa Mungu. 4 Aliamka chakulani na
akatandika chini vazi lake la nje. Kisha alichukua taulo na akajifunga mwenyewe.
5 Kisha akatia maji katika bakuli na akaanza kuwaosha miguu wanafunzi wake
na kuwafuta na taulo ambayo alijifunga yeye mwenyewe. 6 Akaja kwa Simoni
Petro, na Petro akamwambia, "Bwana, Unataka kuniosha miguu yangu?" 7 Yesu
akajibu na kumwambia, "Nifanyalo hulijui sasa, lakini utaelewa baadaye." 8 Petro
akamwambia, "Hutaniosha miguu yangu kamwe." Yesu akamjibu, "Ikiwa sitakuosha,
hutakuwa na sehemu pamoja nami." 9 Simoni Petro akamwambia, "Bwana, usinioshe
miguu yangu tuu, bali pia na mikono na kichwa changu." 10 Yesu akamwambia,
"Yeyote ambaye amekwisha kuoga haitaji kuoga isipokuwa miguu yake, na amekuwa
safi mwili wake wote; ninyi mmekuwa safi, lakini si nyote." 11 Kwa kuwa Yesu
alijua yule atakaye msaliti; hii ndiyo sababu alisema, si nyote mmekuwa safi."
12 Wakati Yesu alipokuwa amewaosha miguu yao na akiisha chukua vazi lake na
kukaa tena, aliwaambia, "Je Mnaelewa kile ambacho nimewafanyia? 13 Mnaniita
mimi "Mwalimu" na Bwana hii mnasema kweli, maana ndivyo nilivyo. 14 Ikiwa
mimi Bwana na mwalimu, nimewaosha miguu yenu, ninyi pia imewapasa kuwaosha
wenzenu miguu. 15 Kwa kuwa nimewapa mfano ili kwamba ninyi pia mfanye kama
mimi nilivyo fanya kwenu. 16 Amini, Amini, nawambia, mtumwa si mkuu kuliko
bwana wake; wala yule ambaye ametumwa ni mkuu kuliko yule aliye mtuma.
17 Ikiwa unafahamu mambo haya, umebarikiwa ukiyatenda. 18 Sisemi kuhusu
ninyi nyote, kwa kuwa nawajua wale ambao nimewachagua - bali nasema haya
ili kwamba maandiko yaweze kutimilizwa: 'Yeye alaye mkate wangu ameniinulia
kisigino chake.' 19 Ninawambia hili sasa kabla halijatokea ili kwamba litakapotokea,
muweze kuamini kuwa mimi NDIYE. 20 "Amini, amini, nawambia, anipokeaye mimi
humpokea ambaye nina mtuma, na yule anipokeaye mimi humpokea yule aliye
nituma mimi." 21 Wakati Yesu aliposema haya, alisumbuka rohoni, alishuhudia na
kusema, "Amini, amini, nawambia kwamba mmoja wenu atanisaliti." 22 Wanafunzi
wake wakatazamana, wakishangaa ni kwa ajili ya nani alizungumza. 23 Kulikuwa
katika meza, mmoja wa wanafunzi wake ameegama kifuani mwa Yesu yule ambaye
Yesu alimpenda. 24 Simoni Petro alimuuliza mwanafunzi huyu na kusema, "Twambie
ni yupi ambaye kwake anazungumza." 25 Mwanafunzi yule aliye egama kifuani mwa
Yesu na akamwambia, "Bwana, ni nani?" 26 Kisha Yesu alijibu, "Ni kwake yule
nitakaye chovya kipande cha mkate na kumpatia." Hivyo alipo kuwa amechovya
mkate, alimpatia Yuda mwana wa Simon Iskariote. 27 Na baada ya mkate, Shetani
alimuingia. Kisha Yesu akamwambia, "Kile ambacho unataka kukifanya ukifanye
haraka." 28 Sasa hakuna mtu katika meza alijua sababu ya Yesu kusema jambo
hili kwake. 29 Baadhi yao walidhani kwamba, kwa sababu Yuda alishika mfuko

wa fedha, Yesu alimwambia, “Nunua vitu tunavyohitaji kwa ajili ya sikukuu,” au
kwamba anapaswa kutoa kitu kwa masikini. 30 Baada ya Yuda kupokea mkate,
alitoka nje harak; na ilikuwa usiku. 31 Wakati Yuda alipokuwa ameondoka, Yesu
alisema, “Sasa mwana wa Adam ametukuzwa, na Mungu ametukuzwa katika yeye.
32 Mungu atamtukuza katika yeye mwenyewe, na atamtukuza haraka. 33 Watoto
wadogo, niko pamoja nanyi kitambo kidogo. Mtanitafuta, na kama nilivyowambia
Wayahudi, 'Niendako, hamuwezi kuja.' sasa nawambia ninyi, pia. 34 Ninawapa amri
mpya, kwamba mpendane; kama mimi nilivyo wapenda ninyi, vivyo hivyo nanyi
pia imewapasa kupendana ninyi kwa ninyi. 35 Kwa ajili ya hili watu watatambua
kuwa ninyi ni wanafunzi wangu, ikiwa mna upendo kwa kila mmoja na mwingine.”
36 Simoni Petro alimwambia, “Bwana, unakwenda wapi?” Yesu akajibu, “Mahali
ninapokwenda kwa sasa hutaweza kunifuata, lakini utanifuata baadaye.” 37 Petro
akamwambia, “Bwana, kwa nini nisikufuate hata sasa? Mimi nitayatoa maisha yangu
kwa ajili yako.” 38 Yesu akajibu, “Je utayatoa maisha yako kwa ajili yangu? Amini
amini nakwambia, jogoo hatawika kabla hujanikana mara tatu.”

# 14

1 “Usiruhusu moyo wako kuwa katika mahangaiko. Unamwamini Mungu niamini
pia na mimi. 2 Katika nyumba ya Baba yangu kuna makazi mengi ya kukaa; kama
isingekuwa hivyo, ningekuwa nimekuambia, kwa vile ninakwenda kukuandalia
mahali kwa ajili yako. 3 Kama nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena
kuwakaribisha kwangu, ili mahali nilipo pia nanyi muwepo. 4 Mnajua njia mahali
ninakoenda.” 5 Tomaso alimwambia Yesu, “Bwana, hatujui mahali unakoenda;
Je! Tunawezaje kuijua njia? 6 Yesu alimwambia, “ Mimi ndiye njia, kweli, na
uzima; hakuna awezaye kuja kwa Baba isipokuwa kupitia kwangu. 7 Kama mngeli
nijua mimi, mngalikuwa mnamjua na Baba yangu pia; kuanzia sasa na kuendelea
mnamjua na mmeshamuona yeye.” 8 Philipo alimwambia Yesu, “Bwana, tuonyeshe
Baba, na hivyo itakuwa imetutosha.” 9 Yesu akamwambia, “Sijakuwa pamoja nanyi
kwa muda mrefu, na bado hunijui mimi, Philipo? Yeyote aliyeniona mimi amemwona
Baba; Jinsi gani unasema, 'Tuonyeshe Baba'? 10 Hamuamini kuwa mimi ni ndani ya
Baba, na Baba yu ndani yangu? Maneno ninayoyasema kwenu sisemi kwa kusudi
langu mwenyewe; badala yake, ni Baba anayeishi ndani yangu anayetenda kazi yake.
11 Niamini mimi, kwamba niko ndani ya Baba, na Baba yuko ndani yangu; kadhalika
niamini mimi kwa sababu ya kazi zangu hasa. 12 Amini, amini, nawaambia, yeye
aniaminiye, mimi kazi zile nizifanyazo, atazifanya kazi hizi pia; na atafanya hata kazi
kubwa kwasababu ninakwenda kwa Baba. 13 Chochote mkiomba katika jina langu,
nitafanya ili kwamba Baba aweze kutukuzwa katika Mwana. 14 Kama mkiomba kitu
chochote katika jina langu, hilo nitafanya. 15 Kama mkinipenda, mtazishika amri
zangu. 16 Na nitamwomba Baba, Naye atawapa Msaidizi mwingine ili kwamba aweze
kuwa pamoja nanyi milele, 17 Roho wa kweli. Ulimwengu hauwezi kumpokea yeye
kwa sababu haumuoni, au kumjwa yeye. hata hivyo ninyi, mnamjua yeye, kwani
anakaa pamoja nayi na atakuwa ndani yenu. 18 Sitawaacha peke yenu; Nitarudi
kwenu. 19 Kwa muda kitambo, ulimwengu hautaniona tena, lakini ninyi mwaniona.
Kwa sababu ninaishi, nanyi mtaishi pia. 20 Katika siku hiyo mtajua kwamba mimi
niko ndani ya Baba, na kwamba ninyi mko ndani yangu, na kwamba mimi niko ndani
yenu. 21 Yeyote azishikaye amri zangu na kuzitenda, ndiye mmoja ambaye anipenda
mimi; na ambaye anipenda mimi atapendwa na Baba yangu, na Nitampenda na
nitajionyesha mimi mwenyewe kwake.” 22 Yuda (siyo Iskariote) akamwambia Yesu,
“Bwana, Je! Ni nini kinatokea kwamba utajionyesha mwenyewe kwetu na siyo kwa
ulimwengu? 23 Yesu alijibu akamwambia, “Kama yeyote danipendaye, atalishika

neno langu. Baba yangu atampenda, na tutakuja kwake na tutafanya makao yetu
pamoja naye. 24 Yeyote ambaye hanipendi mimi, hashiki maneno yangu. Neno
ambalo mnasikia siyo langu bali la Baba ambaye alinituma. 25 Nimeyasema mambo
haya kwenu, wakati bado ninaishi miongoni mwenu. 26 Hata hivyo, Mfariji, Roho
Mtakatifu, ambaye Baba atamtuma kwa jina langu, atawafundisha mambo yote na
atawafanya mkumbuke yote ambayo niliyasema kwenu. 27 Amani nawapa amani
yangu ninyi. Siwapi hii kama ulimwengu utoavyo. Msiifanye mioyo yenu kuwa na
mahangaiko, na woga. 28 Mlisikia vile nilivyowaambia, 'Ninaenda zangu, na nitarudi
kwenu.' Kama mngelinipenda mimi, mngekuwa na furaha kwa sababu ninakwenda
kwa Baba, kwa kuwa Baba ni mkuu kuliko mimi. 29 Sasa nimekwisha kuwaambia
kabla haijatokea ili kwamba, wakati ikitokea, mweze kuamini. 30 Sitaongea nanyi
maneno mengi, kwa kuwa mkuu wa dunia hii anakuja. Yeye hana nguvu juu yangu,
31 lakini ili kwamba ulimwengu upate kujua kwamba nampenda Baba, nafanya
ambacho Baba ananiagiza mimi, kama vile alivyonipa amri. Inukeni, na tutoke
mahali hapa.

# 15

1 Mimi ni mzabibu wa huu kweli, na baba yangu ni mkulima wa mzabibu. 2 Kila
tawi ndani yangu ambalo halizai tunda, na husafisha kila tawi ambalo huzaa tunda
huliondoa ili kwamba liweze kuzaa zaidi. 3 Ninyi tayari mmekuwa safi kwa sababu
ya ujumbe ambao nimekwisha waambia. 4 Mkae ndani yangu, na mimi ndani yenu.
Kama tawi lisivyoweza kuzaa peke yake lisipo kuwa katika mzabibu, kadhalika
nayi, msipo kaa ndani yangu. 5 Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi. Adumuye
ndani yangu na mimi ndani yake, mtu huyu huzaa matunda mengi, kwa kuwa
pasipo mimi hamuwezi kufanya jambo lolote. 6 Ikiwa mtu yeyote hatasalia ndani
yangu, atatupwa kama tawi na kukauka; watu hukusanya matawi na kuyatupa
katika moto, na kuteketea. 7 Ikiwa mtadumu ndani yangu, na kama maneno yangu
yakidumu ndani yenu, ombeni lolote mtakalo, nanyi mtafanyiwa. 8 Katika hili baba
yangu ametukuzwa, kwamba mnazaa matunda mengi na kwamba ni wanafunzi
wangu. 9 Kama baba yangu alivyonipenda mimi, mimi pia nimewapenda ninyi;
dumuni katika pendo langu. 10 Ikiwa mtashika amri zangu, mtadumu katika pendo
langu kama nilivyo shika amri za baba yangu na kudumu katika pendo lake.
11 Nimesema mambo haya kwenu ili kwamba furaha yangu iwe ndani yenu na ili
kwamba furaha yenu ifanyike kuwa timilifu. 12 Hii ndiyo amri yangu, kwamba
mpendane ninyi kwa ninyi kama nilivyo wapenda ninyi. 13 Hakuna mtu aliye na
upendo mkuu kuliko huu, kwamba ayatoe maisha yake kwa ajiliya rafiki zake.
14 Ninyi ni rafiki zangu ikiwa mtafanya yale niwaagizayo. 15 Siwaiti watumwa,
kwa kuwa mtumwa hajui kile afanyacho bwana wake. Nimewaita ninyi marafiki,
kwa sababu nimewajulisheni mambo yote ambayo nimesikia kutoka kwa Baba.
16 Hamkunichagua mimi, bali mimi niliwachagua ninyi na kuwaweka mwende
mazae matunda, na tunda lenu lipate kukaa. Hii liko hivi ili kwamba chochote
muombacho kwa Baba kwa jina langu, atawapeni. 17 Mambo haya ninawaagiza,
kwamba mpendane kila mtu na mwenzake. 18 Kama ulimwengu utawachukia,
mjuwe kwamba ulinichukia mimi kabla haujawachukia ninyi. 19 Kama mngekuwa
wa ulimwengu, ulimwengu ungewapenda kama wa kwao; Lakini kwa sababau
ninyi sio wa ulimwengu na kwa sababu niliwachagua kutoka katika ulimwengu,
ni kwa ajili hii ulimwengu huwachukia. 20 Kumbukeni neno ambalo niliwaambia,
'Mtumwa si mkuu kuliko bwana wake.' Ikiwa walinitesa mimi, watawateseni ninyi
pia; Kama walishika neno langu, wangelishika la kwenu pia. 21 Watawatendeeni
mambo haya yote kwa ajili ya jina langu kwa sababu hawamjui yule aliyenituma.

[22] Kama nisingekuja na kuwaambia waambia, wasingalikuwa wamefanya dhambi;
lakini sasa hawana udhuru kwa dhambi yao. [23] Anichukiaye mimi humchukia Baba
pia. [24] Ikiwa sijafanya kazi miongoni mwao ambayo hapana mmoja aliyeifanya,
wangelikuwa hawana dhambi; lakini sasa wamefanya yote mawili wameona na
wamenichukia mimi na Baba yangu. [25] Hili linatokea ili kwamba neno litimie ambalo
limeandikwa katika sheria yao: 'Wananichukia mimi bila sababu.' [26] Wakati mfariji
amekuja, ambaye nitamtuma kwenu kutoka kwa Baba, huyu ndiye, Roho wa kweli,
ambaye anatokea kwa Baba, atanishuhudia. [27] Ninyi pia mnanishuhudia kwa sababu
mmekuwa pamoja nami tangu mwanzo.

# 16

[1] Nimewaambia mambo haya ili msiweze kukwazwa. [2] Watawatoa nje ya masi-
nagogi; hakika saa inakuja ambayo kila atakayewaua atafikiri kuwa anafanya kazi
njema kwa ajili ya Mungu. [3] Watawatendea mambo haya kwa sababu hawamfahamu
Baba wala hawanifahamu mimi. [4] Nimewaambia mambo haya ili kwamba wakati
ukifika wa haya kutokea, mnaweza kuyakumbuka na jinsi nilivyowaambia muweze
wao. Sikuwaambia kuhusu mambo haya tangu mwanzo kwa sababu nilikuwa
pamoja nanyi. [5] Japokuwa, sasa naenda kwa yule aliyenituma; lakini hakuna
kati yenu anayeniuliza, “Unaenda wapi?” [6] Kwa sababu nimesema maneno haya
kwenu, huzuni imejaa mioyoni mwenu. [7] Hata hivyo, nawaambia ukweli: ni vyema
kwenu nikiondoka; kwa maana nisipoondoka, mfariji hatakuja kwen; lakini nikienda
ntamtuma kwenu. [8] Akija, huyo mfariji ataubitisha ulimwengu kuhusiana na dhambi,
kuhusiana na haki na kuhusiana na hukumu. [9] Kuhusiana na dhambi, kwa sababu
hawakuniamini mimi, [10] kuhusiana na haki, kwa sababu naenda kwa baba, na
hamtaniona tena; [11] na kuhusiana na hukumu kwa sababu mkuu wa ulimwengu huu
amehukumiwa. [12] Ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamtayaelewa sasa. [13] Lakini,
yeye, Roho wa kweli, akija, atawaongoza katika kweli yote; kwa kuwa hataongea
kwa ajili yake mwenyewe; lakini yoyote atakayoyasikia, atayasema mambo hayo; na
atayadhihirisha kwenu mambo yatakayokuja. [14] Yeye atanitukuza mimi, kwa sababu
atayachukua mambo yangu na atayatangaza kwenu. [15] Vitu vyote alivyonavyo
Baba ni vyangu; kwa hiyo, nimesema kwamba Roho atachukua mambo yangu
na atayadhihirisha kwenu. [16] Bado muda mfupi, hamtaniona tena; na baada ya
muda mfupi tena, mtaniona.” [17] Baadhi ya wanafunzi wake wakaambizana, “Ni
nini anachotuambia, “muda mfupi, na hamtaniona tena,' na, kisha, mda mfupi
mtaniona,' na, 'kwa sababu naenda kwa Baba?” [18] Kwa hiyo wakasema, “Ni kitu gani
anachosema, 'Bado mda mfupi'? Hatujui asemavyo.” [19] Yesu aliona kuwa walitamani
kumuuliza, naye akawaambia, “Mnajiuliza wenyewe kuhusu hili, nilivyosema, 'Bado
muda mfupi, hamtaniona tena; na baada ya muda mfupi mtaniona'? [20] Amin,
amin, nawaambia, mtalia na kuomboleza, lakini ulimwengu utashangilia, mtakuwa
na huzuni lakini huzuni yenu itageuka kuwa furaha. [21] Mwanamke anakuwa na
huzuni wakati anapokuwa na uchungu kwa sababu wakati wa kujifungua umefika;
lakini anapojifungua mtoto, hakumbuki tena maumivu kwa sababu ya furaha yake
kwamba mtoto amezaliwa duniani. [22] Ninyi pia mna huzuni sasa, lakini nitawaona
tena; na mioyo yenu itafurahi na hakuna atakayeweza kuiondoa furaha yenu.
[23] Siku hiyo hamtaniuliza maswali. Amin, Amin, nawaambia, Mkiomba lolote kwa
Baba, atawapa kwa jina langu. [24] Mpaka sasa hamjaomba lolote kwa jina langu;
ombeni, nanyi mtapokea ili kwamba furaha yenu ikamilike. [25] Nimezungumza na
ninyi kwa lugha isiyoeleweka, lakini saa inakuja ambapo sitazungumza kwa lugha
isiyoeleweka lakini badala yake nitawaambia waziwazi kuhusu Baba. [26] Siku hiyo
mtaomba kwa jina langu, na siwaambii kwamba nitaomba kwa Baba kwa ajili yenu;

27 Kwa kuwa Baba mwenyewe anawapenda kwa sababu mmenipenda mimi na kwa
sababu mmeniamini kuwa nimetoka kwa Baba. 28 Nilitoka kwa Baba na nimekuja
ulimwenguni; tena, naondoka ulimwenguni na ninaenda kwa Baba". 29 Wanafunzi
wake wakamwambia, "Unaona, sasa unaongea wazi wazi na hautumii mafumbo.
30 Sasa, tunajua kwamba unajua mambo yote, na hauhitaji mtu yoyote akuulize
maswali. Kwa sababu hii tunaamini kuwa unatoka kwa Mungu. 31 Yesu akawajibu,
"Sasa mmeamini?" 32 Tazama, saa inakuja, ndiyo na hakika imefika, ambapo
mtatawanyika kila mmoja na kwa wa kwao mtaniacha mwenyewe. Lakini siko peke
yangu kwa sababu Baba yupo nami. 33 Nawaambia mambo haya ili kwamba ndani
yangu muwe na amani. Duniani mna matatizo, lakini jipeni moyo, nimeushinda
ulimwengu.

# 17

1 Yesu aliyasema mambo haya; kisha akainua macho yake kuelelea mbinguni na
akasema, "Baba, saa imewadia; mtukuze mwanao ili na mwana naye akutukuze
wewe - 2 kama vile ulivyompatia mamlaka juu ya vyote vyenye mwili ili awape
uzima wa milele wale wote uliompatia. 3 Huu ndio uzima wa milele: kwamba
wakujue wewe, Mungu wa kweli na wa pekee, na yeye uliyemtuma, Yesu Kristo.
4 Nilikutukuza hapa duniani, na kuikamilisha kazi uliyonipa niifanye. 5 Sasa, Baba,
unitukuze mimi pamoja na wewe mwenyewe kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja
na wewe kabla ya ulimwengu kuumbwa. 6 Nililifunua jina lako kwa watu ulionipa
hapa duniani. Walikuwa watu wako; lakini ulinikabidhi mimi. nao wamelishika neno
lako. 7 Sasa wanajua kuwa kila kitu ulichonipa mimi kinatoka kwako, 8 kwa maneno
yale uliyonipatia mimi— Nimekwisha wapatia wao maneno hayo. Waliyapokea na
kweli wakajua ya kuwa mimi nimetoka kwako, na wakaamini kuwa wewe ndiye
uliyenituma. 9 Ninawaombea wao. Siuombei ulimwaengu bali wale ulionipa kwa
kuwa wao ni wako. 10 Vitu vyote ambavyo ni vyangu ni vyako, na vile ulivyonavyo
wewe ni vyangu; nami ninatukuzwa katika hivyo. 11 Mimi simo tena ulimwenguni,
bali wao wamo ulimwenguni, nami sasa naja kwako. Baba Mtakatifu, watunze kwa
jina lako lile ulilonipa sisi ili wao nao wawe na umoja, kama vile mimi na wewe
tulivyo na umoja. 12 Nilipokuwa nao, niliwalinda kwa jina ulilonipa; Niliwalinda,
na hakuna hata mmoja wao aliyepotea isipokuwa mwana wa upotevu, ili kwamba
maandiko yatimie. 13 Sasa ninakuja kwako; lakini ninasema haya ulimwenguni
ili kwamba furaha yangu ikamilishwe ndani yao wenyewe. 14 Nimewapa neno
lako; ulimwengu imewachukia kwa sababu wao si wa ulimwengu, kama vile
mimi nisivyokuwa wa ulimwengu 15 Siwaombei kwamba uwatoe ulimwenguni bali
uwalinde na yule mwovu. 16 Wao si wa dunia kama vile mimi nisivyokuwa wa
ulimwenguni. 17 Uwaweke wakfu kwako mwenyewe katika Kweli; neno lako ndiyo
kweli. 18 Ulinituma ulimwenguni, nami nimewatuma ulimwenguni. 19 Kwa ajili
yao mimi mwenyewe ninajitoa kwako ili kwamba na wao wajitoe kwako kwa ile
kweli. 20 Si hawa tu ninaowaombea, bali na wale watakaoamini kupitia neno lao
21 ili kwamba wao nao wawe na umoja, kama vila wewe Baba, ulivyo ndani yangu
nami ndani yako. Nawaombea ili kwamba wao pia waweze kuwa ndani yetu ili
ulimwengu uweze kuamini kuwa wewe ndiye uliyenituma. 22 Utukufu ule ulionipa
mimi - nimewapa wao, ili kwamba waweze kuwa na umoja, kama vile sisi tulivyo
umoja - 23 Mimi ndani yao, nawe ndani yangu, ili waweze kukamilishwa katika umoja;
ili ulimwengu ujue kuwa hakika wewe ndiye uliyenituma, na kuwapenda, kama vile
wewe ulivyonipenda, mimi. 24 Baba, kile ulichonipa mimi - Natamani kwamba wao
pia waweze kuwa pamoja nami mahali nilipo ili waweze kuona utukufu wangu,
ule ulionipa: kwa kuwa wewe ulinipenda mimi kabla ya kuumbwa kwa misingi

ya ulimwengu. 25 Baba mwenye haki, ulimwengu haukukujua wewe, lakini mimi
nakujua wewe; na wanajua kwamba ulinituma. 26 Nililifanya jina lako lijulikane
kwao, na nitalifanya lijulikane ili kwamba lile pendo ambalo kwalo ulinipenda mimi
liweze kuwa ndani yao, na mimi niweze kuwa ndani yao."

## 18

1 Baada ya Yesu kusema maneno haya, aliondoka na wanafunzi wake kuelekea
bonde la Kidron, ambako kulikuwa na bustani, ambako yeye na wanafunzi wake
wakaingia ndani yake. 2 Sasa yule Yuda, aliyetaka kumsaliti, naye alilijua eneo
hilo, kwani Yesu alikuwa akienda hili eneo mara kadhaa akiwa na wanafunzi wake.
3 Naye Yuda, baada ya kuwa amepata kundi la maaskari na maofisa toka kwa wakuu
wa makuhani, wakaja wakiwa na taa, kurunzi na silaha. 4 Naye Yesu, hali akijua
kila kitu kilichokuwa kikifanyika dhidi yake, alijitokeza mbele na akawauliza, "Ni
nani mnayemtafuta?" 5 Nao wakamjibu, "Yesu Mnazareth." Yesu akawaambia,
"Mimi ndiye" Naye Yuda aliyemsaliti, alikuwa amesimama pamoja na wale askari.
6 Kwa hiyo alipowaambia, "Mimi ndiye" walirudi kinyume na kuanguka chini.
7 Halafu akawauliza tena, "Ni nani mnayemtafuta? Nao wakamjibu tena "Yesu
mnazareth." 8 Yesu akawajibu, "Nimekwisha kuwaambia kuwa Mimi ndiye; kwa
hiyo kama mnanitafuta mimi, waacheni hawa wengine waende." 9 Haya yalikuwa
hivyo ili lile neno litimilike; pale aliposema; "Katika wale ulionipa, sikumpoteza
hata mmoja." 10 Ndipo Simon Petro, aliyekuwa na upanga, akaufuta na kumkata
sikio la kulia mtumishi wa Kuhani mkuu. Na jina lake mtumishi yule lilikuwa
Malko. 11 Yesu akamwambia Petro, "Rudisha upanga wako kwenye ala yake. Kwa
nini nisikinywee kikombe kile alichonipa Baba?" 12 Basi lile kundi la askari na
jemedari, na watumishi wa Wayahudi, walimkamata Yesu na kumfunga. 13 Nao
wakamwongoza kwanza mpaka kwa Anasi, kwani yeye alikuwa mkwe wa Kayafa,
ambaye ndiye aliyekuwa Kuhani mkuu kwa mwaka huo. 14 Sasa Kayafa ndiye
aliyekuwa amewapa ushauri Wayahudi ya kwamba ilimpasa mtu mmoja afe kwa
ajili ya watu. 15 Simon Petro alimfuata Yesu, na vivyo hivyo mwanafunzi mwingine.
Na yule mwanafunzi alikuwa akifahamika kwa kuhani mkuu, naye akaingia pamoja
na Yesu katika behewa ya Kuhani mkuu; 16 lakini Petro alikuwa amesimama nje ya
mlango. Basi yule mwanafunzi aliyekuwa akifahamika kwa kuhani mkuu, alitoka
nje akaenda kuongea na yule mwanamke mtumishi aliyekuwa akilinda mlango
na kumwingiza Petro ndani. 17 Basi yule kijakazi aliyekuwa akilinda mlango,
alimwambia Petro, "Je wewe si mmoja wa wafuasi wa huyu mtu?" Naye akasema,
"Mimi siye." 18 Na wale watumishi na wakuu walikuwa wakisimama mahali pale;
wamekoka moto wa kwa maana, kulikuwa na baridi, na hivyo walikuwa wakiota
moto ili kupata joto. Naye Petro alikuwa nao, akiota moto akiwa amesimama.
19 Kuhani mkuu alimhoji Yesu juu ya wanafunzi wake na mafundisho yake. 20 Yesu
akamjbu, "Nimeuambia waziwazi ulimwengu; Mimi nilifundisha mara kwa mara
kwenye masinagogi na hekaluni mahali ambapo wayahudi hukusanyika. Nami
sikusema lolote katika siri. 21 Kwa nini mliniuliza? Waulizeni walionisikiliza juu ya
kile nilichosema. Hawa watu wanajua mambo yale niliyosema. 22 Yesu alipokwisha
sema hivyo, mmoja wa wakuu aliyekuwa amesimama akampiga Yesu kwa mkono
wake na kisha akasema, "Je, hivyo ndivyo inavyokupasa kumjibu kuhani mkuu?"
23 Naye Yesu akamjibu, "Kama nimesema jambo lolote baya basi uwe shahidi kwa ajili
ya uovu, na kama nimemjibu vyema kwa nini kunipiga? 24 Ndipo Anasi alipompeleka
Yesu kwa Kayafa kuhani mkuu akiwa amefungwa. 25 Sasa Simoni Petro alikuwa
amesimama akijipasha joto mwenyewe. Halafu wale watu wakamwambia. "Je, wewe
pia si mmoja wa wanaafunzi wake?" Akakana akisema "Mimi siye." 26 Mmoja wa

watumishi wa kuhani mkuu, ambaye alikuwa ndugu wa yule mwanaume ambaye
Petro alimkata sikio, alisema, “Je si wewe niliyekuona naye kule bustanini?” 27 Petro
akakana tena, na mara Jogoo akawika. 28 Kisha wakamchukua Yesu toka kwa
Kayafa mpaka kwenye Praitorio. Ilikwa asubuhi na mapema. Wao wenyewe
hawakuiingia ile Praitorio ili wasije wakanajisika na kuila pasaka. 29 Kwa hiyo Pilato
akawaendea akisema. “Ni shitaka gani linalomhusu huyu mtu?” 30 Wakamjibu na
kumwambia, “Kama huyu mtu asingekuwa mtenda maovu, tusingemleta kwako.”
31 Pilato akawaambia, “Mchukueni ninyi wenyewe, mkamhukumu kulingana na
sheria yenu.” Nao Wayahudi wakamwambia, “Sheria haituruhusu sisi kumwua mtu
yeyote.” 32 Walisema haya ili neno la Yesu litimilike, neno ambalo alikuwa amekwisha
sema juu ya aina ya kifo chake. 33 Basi Pilato akaingia tena Praitorio akumwita Yesu;
akamwambia, “Je, wewe ni mfalme wa Wayahudi?” 34 Yesu akamjibu, “Je, wewe
waniuliza swali hili kwa Sababu wataka kujua au kwa sababu wengine wamekutuma
ili uniulize mimi?” 35 Naye Pilato akamjibu, “Mimi si Myahudi, au sivyo?” Taifa
lako na kuhani mkuu ndio waliokuleta kwangu; wewe umefanya nini? 36 Yesu
akajibu; “Ufalme wangu si wa ulimwengu huu, kama ufalme wangu ungekuwa na
sehemu katika ulimwengu huu watumwa wangu wangenipigania ili nisitolewe kwa
wayahudi. Kwa kweli ufalme wangu hautoki hapa” Basi 37 Pilato akamwambia,
“Je, wewe basi u mfalme?” Yesu akajibu, “wewe ndivyo unanvyosema kuwa mimi
ni mfalme, Kwa sababu hii mimi nilizaliwa na kwa sababu hii mimi nimekuja
ulimwenguni ili niwe shahidi wa ile kweli. Yeyote aliye wa hiyo kweli huisikiliza
sauti yangu. 38 Pilato akamwambia, “Kweli ni nini?” Naye alipokwisha sema haya
akaenda kwa Wayahudi na kuwaambia “Siona katika lolote mtu huyu. 39 Ninyi
mna utamaduni unaonifanya nimfunfungulie mfungwa mmoja wakati wa Pasaka.
Je mnataka nimfungulie mfalme wa Wayahudi.” 40 Kisha walipiga kelele wakisema,
siyo huyu, tufungulie Baraba.” Naye Baraba alikuwa mnyang'anyi.

# 19

1 Basi Pilato alimchukua Yesu na kumchapa. 2 Wale maaskari wakasokota miiba na
kutengeneza taji. Wakaiweka juu ya kichwa cha Yesu na kumvalisha vazi la rangi ya
zambarau. 3 Wakamjia na kusema, “Wewe mfalme wa Wayahudi! na kisha kumpiga
kwa mikono yao. 4 Kisha Pilato alitoka nje na kuwaambia watu, “Tazama nawaleteeni
huyu mtu kwenu ili mjue kwamba mimi sikuona hatia yoyote ndani yake.” 5 Kwa
hiyo Yesu akatoka nje; alikuwa amevaa taji ya miiba na vazi la zambarau. Ndipo
Pilato akawaambia, “Tazameni mtu huyu hapa!” 6 Kwa hiyo wakati kuhani mkuu na
wakuu walipomwona Yesu, wakapiga kelele wakisema, “Msulubishe, msulubishe.”
Pilato akawaambia, “Mchukueni ninyi wenyewe mkamsulubishe, kwa kuwa mimi
sioni hatia ndani yake.” 7 Wayahudi wakamjibu Pilato, “Sisi tunayo sheria, na
kwa sheria hiyo inampasa kufa kwa sababu yeye alijifanya kuwa mwana wa
Mungu.” 8 Pilato aliposikia maneno haya alizidi kuogopa, 9 akaingia Praitorio tena na
kumwambia Yesu, “Wewe unatoka wapi? Hata hivyo, Yesu hakumjibu. 10 Kisha Pilato
akamwambia, “Je, wewe huongei na mimi? Je, wewe hujui kuwa mimi nina mamlaka
ya kukufungua na mamlakaya kukusulubisha?” 11 Yesu akamjibu, “Usingekuwa na
nguvu dhidi yangu kama usingepewa toka juu. Kwa hiyo, mtu aliyenitoa kwako
ana dhambi kubwa.” 12 Kutokana na jibu hili, Pilato akataka kumwacha huru,
lakini Wayahudi wakapiga kelele wakisema, “Kama utamwacha huru basi wewe
si rafiki wa Kaisari: Kila ajifanyaye kuwa mfalme hunena kinyume cah kaisari.”
13 Pilato alipoyasikia maneno haya, akamleta Yesu nje kisha akakaa kwenye kiti cha
hukumu mahali pale panapojulikana kama sakafu, lakini kwa Kiebrania, Gabatha.
14 Siku ya maandalizi ya pasaka ilipofika, panapo muda wa saa ya sita. Pilato

akawaambia Wayahudi, “Tazameni mfalme wenu huyu hapa!” 15 Wakapiga kelele,
“Mwondoshe, mwondoshe, msulubishe!” Pilato akawaambia, “Je, nimsulubishe
mfalme wenu?” Naye Kuhani mkuu akajibu, “Sisi hatuna mfalme isipokuwa Kaisari.”
16 Ndipo Pilato alipomtoa Yesu kwao ili asulibiwe. 17 Nao wakamchukua Yesu, naye
akatoka, hali ameubeba msalaba wake mwenyewe mpaka kwenye eneo liitwalo
fuvu la kichwa, kwa Kihebrania huitwa Golgotha. 18 Ndipo walipomsulibisha Yesu,
pamoja naye wanaume wawili, mmoja upende huu na mwingine upande huu, na
Yesu katikati yao. 19 Kisha Pilato akaandika alama na kuiwekwa juu ya msalaba.
Hapo paliandikwa: YESU MNAZARETH, MFALME WA WAYAHUDI. 20 Wengi wa
Wayahudi waliisoma alama hiyo kwani mahali pale aliposulibishwa Yesu palikuwa
karibu na mji. Alama hiyo iliadikwa kwa Kiebrania, kwa Kirumi na kwa Kiyunani.
21 Kisha wakuu wa makuhani wa Wayahudi wakamwambia Pilato, “Usiandike,
'Mfalme wa Wayahudi; bali yeye alisema mimi ni mfalme wa Wayahudi.” 22 Naye
Pilato akawajibu, “Niliyoandika nimeandika.” 23 Baada ya askari kumsulibisha
Yesu, walichukua mavazi yake na kuyagawa katika mafungu manne, kila askari
fungu moja, vivyo hivyo na kanzo, Sasa ile kanzu haikuwa imeshonwa bali ilkuwa
imefumwa yote tokea juu. 24 Kisha wakasemezana wao kwa wao, “Tusiipasue, bali
tupigeni kura ili kuona itakuwa ya nani.” Hili lilitokea ili lile andiko litimizwe,
lile lisemalo waligawanya nguo zangu, na vazi langu wakalipigia kura.” 25 Askari
walifanya mambo haya. Mama yake Yesu, dada wa mama yake, Mariamu mke wa
Kleopa na Mariamu Magdalena - wanawake hawa walikuwa wamesimama karibu
na msalaba wa Yesu. 26 Yesu alipomwona mama yake pamoja na yule mwanafunzi
aliyempenda wakisimama karibu, akamwambia mama yake, “Mwanamke, tazama,
ona mwanao huyu hapa!” 27 Kisha akamwambia yule mwanfunzi, “Tazama, huyu
hapa mama yako. “Tokea saa hiyo yule mwanafunzi akamchukua kwenda nyumbani
kwake. 28 Baada ya hilo, Hali Yesu akijua kuwa yote yamekwisha kumalizika ili
kutimiza maandiko, akasema, “Naona kiu.” 29 Chombo kilichokuwa kimejaa Siki
kilikuwa kimewekwa pale, kwa hiyo wakaweka sifongo iliyojaa siki juu ya ufito
wa hisopo, wakamwekea mdomoni mwake. 30 Naye Yesu alipoionja hiyo, akasema,
“Imekwisha.” Kisha akainamisha kichwa chake, akaikabidhi roho yake. 31 Kwa vile
ilikuwa ni wakati wa maandalio, na kwa sababu miili haikutakiwa kubaki juu ya
msalaba wakati wa Sabato (kwa kuwa Sabato ilikuwa siku ya muhimu), wayahudi
walimwomba Pilato kuwa miguu yao wale wliokuwa wamesulibishwa ivunjwe, na
kwamba miili yao ishushwe. 32 Ndipo askari walipokuja na kuvunja miguu ya mtu
wa kwanza na wa pili aliyekuwa amesulibiwa pamoja na Yesu. 33 Walipomfikia
Yesu, walimkuta tayari alikuwa amekwisha kufa, kwa hiyo hawakuvunja miguu
yake. 34 Hata hivyo, mmoja wa askari alimchoma Yesu ubavuni kwa mkuki, na mara
yakatoka maji na damu. 35 Naye aliyeona hili ametoa ushuhuda, na ushuhuda wake
ni wa kweli. Yeye anajua kuwa alichokisema ni cha kweli ili nanyi pia muamini.
36 Mambo haya yalikuwa ili lile neno lililonenwa lipate kutimia, “Hakuna hata
wake mmoja utakaovunjwa.” 37 Tena andiko lingine husema, “Watamtazama yeye
waliyemchoma” 38 Baada ya mambo haya Yusufu wa Arimathaya, kwa vile alikuwa
mwanafunzi wa Yesu, lakini kwa siri kwa kuwaogopa Wayahudi, alimwomba Pilato
kwamba auchukue mwili wa Yesu. Naye Pilato akampa ruhusa. Kwa hiyo Yusufu
akaja kuuondoa mwili wa Yesu. 39 Naye Nicodemo ambaye hapo awali alimfuata
Yesu usiku naye akaja. Yeye alileta mchanganyiko wa manemane na udi, yapata uzito
wa ratili mia moja. 40 Kwa hiyo wakauchukua mwili wa Yesu wakaufanga kwenye
sanda ya kitani na pamoja na yale manukato, kama ilivyokuwa desturi ya wayahudi
wakati wa kuzika. 41 Mahali ambapo Yesu alisulibiwa kulikuwa na bustani; ndani ya
ile bustani kulikuwa na kaburi jipya ambalo hakuna mtu alikuwa amawahi kuzikwa

humo. 42 Basi, kwa kuwa ilikuwa siku ya maandalio kwa Wayahudi, na kwa vile lile
kaburi lilikuwa karibu, basi wakamlaza Yesu ndani yake.

# 20

1 Mapema siku ya kwanza ya juma, kungali bado giza, Mariamu Magdalena
alikuja kaburini; akaliona lile jiwe limeondolewa kaburini. 2 Kwa hiyo akakimbia
mbio kwenda kwa Simon Petro na kwa yule mwanafunzi mwingine ambaye Yesu
alimpenda, kisha akawaambia, “wamemchukua Bwana kaburini, nasi hatujui kule
walikomlaza.” 3 Kisha Petro na yule mwanafunzi mwingine wakatoka, kuelekea
kaburini. 4 Wote walipiga mbio kwa pamoja; yule mwanafunzi mwingine alikimbia
kwa kasi zaidi ya Petro nakufika kaburini wa kwanza. 5 Akasimama na kisha
kuangalia kaburini; akaiona ile sanda ya kitani imelala, lakini hakuingia ndani.
6 Kisha Simon Petro naye akafika akaingia ndani ya Kaburi. Akaiona ile sanda ya
kitani imelala pale 7 na ile leso iliyokuwa kichwani pake haikuwa imelala pamoja na
zile sanda za kitani bali ilikuwa imelala pembeni peke yake. 8 Ndipo yule mwanafunzi
mwingine naye alipoingia ndani ya kaburi; akaona na kuamini. 9 Kwa kuwa hadi
wakati huo walikuwa bado hawajayajua maandiko kwamba ilimlazimu Yesu afufuke
tena katika wafu. 10 Kisha wanafunzi wakaenda tena nyumbani kwao. 11 Hata
hivyo, Mariamu alikuwa amesimama kaburini akilia, alivyokuwa akiendelea kulia
alisimama kisha akatazama kaburini. 12 Akaona malaika wawili wenye sura nyeupe
wamekaa mmoja kichwani na mwingine miguuni mahali ambapo Yesu alikuwa ame-
lala. 13 Nao wakamwambia, “Mwanamke, kwa nini unalia?” Naye akawaambia, “Ni
kwa sababu wamemchukua Bwana wangu, nami sijui walikomweka.” 14 Alipokwisha
sema hayo, aligeuka na kumwona Yesu akiwa amesimama. Lakini hakutambua kama
huyo alikuwa Yesu. 15 Naye Yesu akamwambia, “Mama, kwa nini unalia? Unamtafuta
nani?” Naye huku akidhani kuwa ni mtunza bustani akamwambia, “Bwana,
kama ni wewe uliyemchukua, niambie ulikomweka, nami nitamchukua.” 16 Yesu
akamwambia, “Mariamu.” Naye akageuka mwenyewe na kumwambia kwa Kiaramu,
“Raboni,” yaani hii ni kusema, “Mwalimu.” 17 Yesu akamwambia, “Usiniguse, kwani
bado sijapaa kwenda kwa baba; bali uende kwa ndugu zangu ukawaambie kuwa
nitapaa kwenda kwa Baba yangu ambaye pia ni Baba yenu, Mungu wangu na Mungu
wenu.” 18 Mariamu Magdalena akaja kuwaambia wanafunzi, “Nimemwona Bwana,”
na kwamba amemwambia mambo haya. 19 Na ilipokuwa jioni, siku hiyo, siku ya
kwanza ya juma, na milango ikiwa imefungwa mahali wanafunzi walipokuwapo
kwa kuwahofia Wayahudi, Yesu alikuja na kusimama katikati yao na kuwaambia,
“Amani iwe kwenu.” 20 Alipokwisha sema haya akawaonesha mikono yake na ubavu
wake. Nao wanafunzi walipomwona Bwana walifurahi. 21 Kisha Yesu akawaambia
tena, “Amani iwe nanyi. Kama vile Baba alivyonituma mimi, vivyo hivyo nami
nawatuma ninyi.” 22 Yesu alipokwisha sema hayo, akawavuvia akawaambia,
Pokeeni Roho Mtakatifu. 23 Yeyote mmsameheye dhambi, wamesamehewa; na
wale mtakaowafungia watafungiwa.” 24 Thomaso, mmoja wa wale kumi na wawili,
aliyeitwa Didimas, hakuwa na wanafunzi wenzake Yesu alipokuja. 25 Wale wanafunzi
wengine waka mwambia baadaye, “Tumemwona Bwana.” Naye akawambia, “Kama
sitaona alama za misumari katika mikono yake, na kuweka vidole vyangu kwenye
hizo alama, na pia kuweka mkono wangu kwenye ubavu wake sitaamini.” 26 Baada
ya siku nane wanafunzi walikuwa chumbani tena, naye Thomaso alikuwa pamoja
nao. Wakati milango ilipokuwa imefungwa Yesu alisimama katikati yao. na akasema,
“Amani na iwe nanyi.” 27 Kisha akamwambia Thomaso, leta kidole chako na uone
mikono yangu; leta hapa mikono yako na uweke kwenye ubavu wangu; wala usiwe
asiyeamini bali aaminiye.” 28 Naye Thomaso akajibu na kumwambia, “Bwana

wangu na Mungu wangu." [29] Yesu akamwambia, Kwa kuwa umeniona, umeamini.
Wamebarikiwa wao wanaoamini, pasipokuona." [30] Kisha Yesu alifanya ishara nyingi
mbele ya wanafunzi, ambazo hazijawahi kuandikwa katika kitabu hiki; [31] bali hizi
zimeandikwa ili kwamba muweze kuamini kwamba Yesu ndiye Kristo, mwana wa
Mungu, na kwamba muaminipo muwe na uzima katika jina lake.

## 21

[1] Baada ya mambo hayo Yesu alijidhihirisha tena kwa wanafunzi katika Bahari
ya Tiberia; hivi ndivyo alivyojidhihirisha mwenyewe: [2] Simon Petro alikuwa
pamoja na Thomaso aitwaye Didimas, Nathanaeli wa kana ya Galilaya, wana wa
Zebedayo na wanafunzi wengine wawili wa Yesu. [3] Simon Petro akawaambia,
"Mimi naenda kuvua samaki." Nao wakamwambia, "Sisi, pia tutaenda nawe."
Wakaenda wakaingia kwenye mashua, lakini usiku huo wote hawakupata chochote.
[4] Na asubuhi kulipokucha, Yesu alisimama ufukweni, nao wanafunzi hawakutambua
kuwa alikuwa Yesu. [5] Kisha Yesu akawambia, "Vijana, mna chochote cha kula?"
Nao wakamjibu, "Hapana." [6] Akawambia, "Shusheni wavu upande wa kuume
wa mashua, nanyi mtapata kiasi." Kwa hiyo wakashusha wavu nao hawakuweza
kulivuta tena kwa sababu ya wingi wa cha samaki. [7] Basi yule mwanafunzi ambaye
Yesu alimpenda akamwambia Petro, "Ni Bwana." Naye Simon Petro aliposikia kuwa
ni Bwana, akajifunga vazi lake (maana hakuwa amelivaa vizuri), kisha akajitupa
baharini. [8] Wale wanafunzi wengine wakaja kwenye mashua (kwani hawakuwa
mbali na pwani, yapata mita mia moja kutoka ufukweni), nao walikuwa wakivuta
zile nyavu zilizokuwa zimejaa samaki. [9] Walipofika ufukweni, waliona moto wa mkaa
pale na juu yake kulikuwa na samaki pamoja na mkate. [10] Yesu akawambia, "Leteni
baadhi ya samaki mliovua sasa hivi." [11] Basi Simon Petro akapanda na kuukokota ule
wavu uliokuwa umejaa samaki wakubwa, kiasi cha samaki 153; japo walikuwa wengi,
ule wavu haukuchanika. [12] Yesu akawaambia, "Njoni mpate kifungua kinywa."
Hakuna hata mmoja wa wanfunzi aliyethubutu kumwuliza, "Wewe ni nani?" Walijua
kuwa alikuwa ni Bwana. [13] Yesu akaja, akachukua ule mkate, kisha akawapa,
akafanya vivyo hivyo na kwa wale samaki. [14] Hii ilikuwa mara ya tatu kwa Yesu
kujidhihirisha kwa wanafunzi wake baada ya kufufuka toka wafu. [15] Baada ya
kuwa wamefungua kinywa, Yesu akamwambia Simon Petro, "Simon mwana wa
Yohana je, wanipenda mimi kuliko hawa?" Petro akajibu, "Ndiyo, Bwana; "Wewe
wajua kuwa mimi nakupenda." Yesu akamwambia, "Lisha wanakondoo wangu."
[16] Akamwambia mara ya pili, "Simon mwana wa Yona, je, wanipenda?" Petro
akamwambia, "Ndiyo, Bwana; wewe wajua kuwa nakupenda. "Yesu akamwambia,
"Chunga kondoo wangu." [17] Akamwambia tena mara ya tatu, "Simon, mwana wa
Yohana, Je wanipenda?" Naye Petro alihuzunika kwa vile alivyomwambia mara ya
tatu, "Je Wewe wanipenda?" Naye akamwambia, "Bwana, unajua yote; unajua kuwa
nakupenda." Yesu akamwambia, Lisha kondoo wangu. [18] Amini, amini, nakuambia,
ulipokuwa kijana ulizoea kuvaa nguo mwenyewe na kwenda kokote ulikotaka; lakini
utakapokuwa mzee, utanyosha mikono yako, na mwingine atakuvalisha nguo na
kukupeleka usikotaka kwenda." [19] Yesu alisema haya ili kuonesha ni aina gani ya kifo
ambacho Petro angemtukuza Mungu. Baada ya kuwa amesema haya, akamwambia
Petro, "Nifuate." [20] Petro aligeuka na kumwona yule mwanafunzi ambaye Yesu
alimpenda akawafuata- Huyu ndiye aliyekuwa amajiegemeza kwenye kifua cha Yesu
wakati wa chakula cha jioni na kumwuliza, "Bwana, ni nani atakayekusaliti?" [21] Petro
alimwona na kisha akamwuliza Yesu, "Bwana, Huyu mtu atafanya nini?" [22] Yesu
akamjibu, "Kama nataka abaki mpaka nitakapokuja, hilo linakuhusu nini?" Nifuate."
[23] Kwa hiyo habari hii ikaenea miongoni mwa wale ndugu, kwamba mwanafunzi

huyo hatakufa. Lakini Yesu hakumwambia Petro kuwa, mwanafunzi huyo hafi,
“Kama nataka yeye abaki mpaka nitakapokuja yakuhusu nini?” 24 Huyu ndiye
mwanafunzi atoaye ushuhuda wa mambo haya, na ndiye aliye andika mambo haya,
na tunajua ya kuwa ushuhuda wake ni kweli. 25 Kuna mambo mengine mengi
ambayo Yesu aliyafanya. Kama kila moja lingeandikwa, nadhani kwamba ulimwengu
wenyewe usingetosha kuviweka vitabu ambavyo vingeandikwa.

# Matendo ya Mitume

1 Kitabu cha zamani nilikiandika, Theofilo, nikisema yote Yesu aliyoanza kufanya
na kufundisha, 2 mpaka siku ambayo Yeye alipokelewa juu. Hii ilikuwa baada ya
kutoa amri kupitia Roho Mtakatifu kwa mitume aliokuwa amewachagua. 3 Baada ya
mateso yake, Yeye alionekana kwao akiwa hai pia na vithibitisho vingi vikishuhudia.
Kwa siku arobaini alijidhihirisha kwao, na alizungumza kuhusu ufalme wa Mungu.
4 Alipokuwa akikutana pamoja nao, aliwaamuru wasiondoke Yerusalemu, lakini
wasubiri kwa ajili ya ahadi ya Baba, ambayo, alisema, “Mlisikia kutoka kwangu
5 kwamba Yohana alibatiza kabisa kwa maji, lakini mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu
katika siku hizi chache.” 6 Na walipokuwa wamekutanika pamoja walimuuliza,
“Bwana, hivi huu ndio muda utakaowarudishia Israeli ufalme?” 7 Yeye akawaambia,
“Siyo sawa kwenu kujua wakati au majira ambayo Baba amekusudia kwa mamlaka
yake mwenyewe.” 8 Lakini mtapokea nguvu, wakati Roho Mtakatifu atakapokuja
juu yenu, na ninyi mtakuwa mashahidi wangu kote katika Yerusalemu na Uyahudi
yote na Samaria mpaka mwisho wa nchi.” 9 Bwana Yesu alipokwisha yasema haya,
wakiwa wanatazama juu, Yeye aliinuliwa juu, na wingu likamfunika wasimwone
kwa macho yao. 10 Wakati wanatazama mbinguni kwa makini akienda, ghafla, watu
wawili walisimama katikati yao wamevaa mavazi meupe. 11 Walisema, “Enyi watu
wa Galilaya, kwa nini mnasimama hapa mkitazama mbinguni?” Huyu Yesu aliyepaa
juu mbinguni atarudi kwa namna ile ile kama mlivyomuona akienda mbinguni.
12 Ndipo wakarudi Yerusalemu kutoka kwenye mlima wa mizeituni, ambao uko
karibu na Yerusalemu, mwendo wa siku ya Sabato. 13 Walipofika walikwenda
ghorofani walikokuwa wakikaa. Nao ni Petro, Yohana, Yakobo, Andrea, Filipo,
Thomaso, Batholomayo, Mathayo, Yakobo Mwana wa Alfayo, Simoni Zelote na Yuda
Mwana wa Yakobo. 14 Wote waliungana kama mtu mmoja, kwa juhudi walikuwa
wakiendelea katika maombi. Pamoja na hao walikuwepo wanawake, Mariamu Mama
yake Yesu, na kaka zake. 15 Katika siku zile Petro alisimama katikati ya ndugu,
kama watu 120, akasema, 16 Ndugu, ilikuwa lazima kwamba maandiko yatimizwe,
ambapo zamani Roho Mtakatifu alisema kwa kinywa cha Daudi kuhusiana na Yuda,
ambaye aliwaelekeza wale waliomkamata Yesu. 17 Kwa kuwa yeye alikuwa mmoja
wetu na alipokea fungu lake la faida katika hii huduma.” 18 (Sasa mtu huyu
alinunua eneo kwa kile alichokipokea kwa uovu wake na hapo alianguka akitanguliza
kichwa, mwili ukapasuka na matumbo yake yote yakawa wazi yakamwagika. 19 Wote
walioishi Yerusalemu walisikia kuhusu hili, hivyo eneo hilo wakaliita kwa lugha yao
“Akeldama” hilo ni “shamba la damu.”) 20 “Kwenye kitabu cha Zaburi imeandikwa,
'Ngoja eneo lake liwe hame na isiruhusiwe hata mmoja kuishi pale;' na, 'Ruhusu mtu
mwingine achukue nafasi yake ya uongozi.' 21 Hiyo ni muhimu, kwa hiyo, mmoja wa
wanaume ambao waliambatana nasi wakati Bwana Yesu alipotoka na kuingia kati
yetu, 22 kuanzia kwenye ubatizo wa Yohana mpaka siku ile alipotwaliwa juu, lazima
awe shahidi wa ufufuo pamoja nasi. 23 “Wakaweka mbele wanaume wawili, Yusufu
aitwaye Barnaba, ambaye pia aliitwa Yusto na Mathia. 24 Wao waliomba wakisema,
“Wewe, Bwana, ujuaye mioyo ya watu wote, hivyo weka wazi yupi kati ya wawili
hawa ambaye umemchagua 25 kuchukua nafasi katika huduma na utume, ambapo
Yuda alitenda uovu na kwenda mahali pake.” 26 Wakapiga kura kwa ajili yao, na
kura ikamwangukia Mathia ambaye alihesabiwa pamoja na wale mitume kumi na
moja.

# 2

1 Ilipofika siku ya Pentekoste, wote walikuwa pamoja sehemu moja. 2 Ghafla
ikatokea muungurumo kutoka mbinguni kama upepo mkali. ukaijaza nyumba
yote walimokuwa wameketi. 3 Hapo zikawatokea ndimi, kama ndimi za moto
zimegawanyika, zikawa juu yao kila mmoja wao. 4 Wao wote wakajazwa na Roho
Mtakatifu na wakaanza kusema kwa lugha zingine, kama vile Roho alivyowajalia
kusema. 5 Sasa walikuwapo wayahudi waliokuwa wanaishi Yerusalemu, wacha
Mungu, kutoka kila taifa chini ya mbingu. 6 Ngurumo hizi ziliposikiwa, kundi la watu
likaja pamoja na wakiwa na wasiwasi kwa sababu kila mtu aliwasikia wakiongea
kwa lugha yake mwenyewe. 7 waliduwaa na kushangazwa, wao walisema, "Kweli,
hawa wote wanaoongea siyo Wagalilaya? 8 Kwa nini sisi tunawasikia, kila mmoja
katika lugha tulizozaliwa nazo? 9 Waparthia na Wamedi na Waelamu, na hao waishio
Mesopotamia, Uyahudi, na Kapadokia, na katika Ponto na Asia, 10 katika Frigia,
Pamfilia, katika Misri, na sehemu ya Libya hata Kirene, na wageni kutoka Rumi,
11 Wayahudi na waongofu, Wakrete na Waarabu, tunawasikia wakizungumza katika
lugha zetu kuhusu kazi za uweza wa Mungu." 12 Wote walikuwa wameduwaa na
kutatanishwa; walisemezana wao kwa wao, "Hii ina maana gani?" 13 Lakini wengine
walidhihaki wakisema, "Hawa wamejazwa kwa mvinyo mpya." 14 Lakini Petro
akasimama pamoja na wale kumi na mmoja, akapaza sauti, akawaambia, "Watu
wa Yudea na wote mnaoishi hapa Yerusalemu, hili lijulikane kwenu, sikilizeni kwa
makini maneno yangu. 15 Watu hawa hawajalewa kama mnavyodhani, sababu saa
hizi ni asubuhi saa tatu. 16 Lakini hili lilikuwa limesemwa kupitia kwa nabii Yoeli:
17 Itakuwa katika siku za mwisho; Mungu asema, nitamwaga Roho wangu kwa watu
wote. Wana wenu na binti zenu watatoa unabii, vijana wenu wataona maono, na
wazee wenu wataota ndoto. 18 Vilevile juu ya watumishi wangu na watumishi wangu
wa kike katika siku hizo, nitamwaga Roho wangu, nao watatabiri. 19 Nitaonesha
maajabu juu angani na ishara chini duniani, damu, moto, na mafusho ya moshi.
20 Na jua litabadilishwa kuwa giza na mwezi kuwa damu, kabla haijaja siku kuu na
ya ajabu ya Bwana. 21 itakuwa ya kwamba kila mmoja ambaye huliitia jina la Bwana
ataokoka.' 22 Watu wa Israeli, sikieni maneno haya: Yesu wa Nazareti, mwanadamu
aliyethibitishwa na Mungu kwenu kwa matendo ya uweza na maajabu, na ishara
ambazo Mungu kupitia Yeye katikati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua- 23 Kwa
sababu ya mpango uliokusudiwa tangu mwanzo, na maarifa ya Mungu, alitolewa, na
ninyi, kwa mikono ya watu wahalifu, mlimsulibisha na kumuua, 24 ambaye Mungu
alimwinua, akauondoa uchungu wa mauti kwake, kwasababu haikuwezekana kwake
kumilikiwa na huo. 25 Hivyo Daudi anasema kuhusu yeye, 'Nilimwona Bwana daima
mbele ya uso wangu, yeye yuko mkono wangu wa kulia hivyo basi sitasogezwa.
26 Kwa hiyo moyo wangu ulikuwa na furaha na ulimi wangu ulifurahishwa. Pia
mwili wangu utaishi katika ujasiri. 27 Hutaiacha nafsi yangu iende kuzimu, wala
hutaruhusu Mtakatifu wako kuona uozo. 28 Wewe umedhihirisha kwangu njia za
uzima; utanifanya nijae furaha mbele ya uso wako.' 29 Ndugu, ninaweza kuzungumza
kwenu kwa ujasiri kuhusu baba yetu Daudi: yeye alikufa na akazikwa, na kaburi
lake liko pamoja nasi hata hivi leo. 30 Hivyo, alikuwa nabii na alijua kuwa Mungu
alishaapa kwa kiapo kwake, kwamba ataweka mmoja katika uzao wake kwenye kiti
cha enzi. 31 Aliliona hili mapema, na akasema kuhusu ufufuo wa Kristo, 'wala alikuwa
hakuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuoza.' 32 Huyu Yesu - Mungu alimfufua,
ambaye sisi wote ni mashahidi. 33 Kwa hiyo, akiwa ameinuliwa katika mkono wa
kuume wa Mungu, na akiwa amepokea ahadi ya Roho Mtakatifu kutoka kwa Baba,
yeye amemimina hii ahadi, ambaye ninyi mnaona na kusikia. 34 Kwani Daudi
hakupaa kwenda mbinguni, lakini anasema, 'BWANA alisema kwa Bwana wangu,

35 “keti mkono wangu wa kulia, mpaka nitakapowafanya adui zako kigoda kwa ajili
ya miguu yako. 36 Kwa hiyo nyumba yote ya Israeli na ijue kwa hakika kwamba
Mungu amemfanya Yeye kuwa Bwana na Kristo, huyu Yesu ambaye mlimsulibisha.”
37 Sasa waliposikia hivyo, wakachomwa katika mioyo yao, wakamwambia Petro
na mitume wengine, “Ndugu, tufanyeje?” 38 Na Petro akawaambia, “Tubuni na
Mbatizwe, kila mmoja wenu, katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya msamaha wa
dhambi zenu, na mtapokea zawadi ya Roho Mtakatifu. 39 Kwani kwenu ni ahadi
na kwa watoto wenu na kwa wale wote walioko mbali, watu wengi kwa kadri
Bwana Mungu wetu atakavyowaita.” 40 Kwa maneno mengi alishuhudia na kuwasihi;
alisema, “Jiokoeni mtoke katika kizazi hiki kiovu.” 41 Ndipo wakayapokea maneno
yake na wakabatizwa, hapo wakaongezeka katika siku hiyo kama nafsi elfu tatu.
42 Wakaendelea katika mafundisho ya mitume na ushirikiano, katika kuumega mkate
na katika maombi. 43 Hofu ikaja juu ya kila nafsi, na maajabu mengi na ishara
zikafanyika kupitia mitume. 44 Wote walioamini walikuwa pamoja na kuwa na vitu
vyao kwa pamoja, 45 na waliuza vitu na milki zao na kugawanya kwa wote kulingana
na hitaji la kila mmoja. 46 Hivyo siku baada ya siku waliendelea wakiwa na lengo
moja katika hekalu, na walimega mkate kwenye kaya, na walishiriki chakula kwa
furaha na unyenyekevu wa moyo; 47 walimsifu Mungu na wakiwa na kibali na watu
wote. Bwana aliwaongeza siku kwa siku ambao walikuwa wakiokolewa.

# 3

1 Sasa Peter na Yohana walikuwa wanaelekea katika hekalu wakati wa maombi,
saa tisa. 2 Mtu fulani, kiwete tangu kuzaliwa, alikuwa akibebwa kila siku na
alikuwa akilazwa katika mlango wa hekalu uitwao mzuri, ili aweze kuomba sadaka
kutoka kwa watu waliokuwa wakielekea hekaluni. 3 Alipowaona Petro na Yohana
wanakaribia kuingia hekaluni, aliomba sadaka. 4 Petro, akimkazia macho, pamoja
na Yohana, alisema,”tutazame sisi.” 5 Kiwete akawatazama, akitazamia kupokea
kitu fulani kutoka kwao. 6 Lakini Petro akasema, “fedha na dhahabu mimi sina,
lakini kile nilichonacho nitatoa kwako. Katika jina la Yesu Kristo wa Nazareth,
tembea.” 7 Petro akamchukua kwa mkono wake wa kulia, na akamwinua juu:
mara moja miguu yake na vifundo vya mifupa yake vikapata nguvu. 8 Akiruka
juu, mtu kiwete alisimama na akaanza kutembea; akaingia hekaluni pamoja na
Petro na Yohana, akitembea, akiruka, na kumsifu Mungu. 9 Watu wote walimwona
akitembea na akimsifu Mungu. 10 Wakatambua kwamba alikuwa ni yule mtu
ambaye alikuwa akikaa akiomba sadaka kwenye mlango mzuri wa hekalu; walijawa
na mshangao na kustaajabu kwa sababu ya kile kilichotokea kwake. 11 Namna
alivyokuwa amewashikilia Petro na Yohana, watu wote kwa pamoja wakakimbilia
kwenye ukumbi uitwao wa Sulemani, wakishangaa sana. 12 Petro alipoliona hili,
yeye akawajibu watu, “Enyi watu wa Israel, kwa nini mnashangaa? Kwa nini
mnayaelekeza macho yenu kwetu, kama kwamba tumemfanya huyu atembee kwa
nguvu zetu wenyewe au uchaji wetu?.” 13 Mungu wa Ibrahimu, na wa Isaka, na
wa Yakobo, Mungu wa Baba zetu, amemtukuza mtumishi wake Yesu. Huyu ndiye
ambaye ninyi mlimkabidhi na kumkataa mbele ya uso wa Pilato, japo yeye alikuwa
ameamua kumwachia huru. 14 Mlimkataa Mtakatifu na Mwenye Haki, na badala yake
mkataka muuaji aachwe huru. 15 Ninyi mlimuua Mfalme wa uzima, ambaye Mungu
alimfufua kutoka kwa wafu - Sisi ni mashahidi wa hili. 16 Sasa, kwa imani katika
jina lake, mtu huyu ambaye mnamwona na kujua, alifanywa kuwa na nguvu. Imani
ambayo inapitia kwa Yesu imempa yeye afya hii kamilifu, mbele yenu ninyi nyote.
17 Sasa, Ndugu, najua kwamba mlitenda katika ujinga, ndivyo pia walivyofanya
viongozi wenu. 18 Lakini mambo ambayo Mungu aliwaambia mapema kwa vinywa

vya manabii wote, kwamba huyu Kristo atateseka, sasa ameyatimiza. 19 Kwa hiyo,
tubuni na mgeuke, ili kwamba dhambi zenu ziweze kuondolewa kabisa, kusudi
zije nyakati za kuburudika kutokana na uwepo wa Bwana; 20 na kwamba aweze
kumtuma Kristo ambaye ameshateuliwa kwa ajili yenu, Yesu. 21 Yeye ndiye ambaye
lazima mbingu zimpokee mpaka wakati wa kurejeshwa kwa vitu vyote, ambavyo
Mungu alizungumzia zamani za kale kwa vinywa vya manabii watakatifu. 22 Hakika
Musa alisema, 'Bwana Mungu atainua nabii kama mimi kutoka katika ndugu zenu.
Mtamsikiliza kila kitu ambacho atawaambia ninyi. 23 Itatokea kwamba kila mtu
ambaye hasikilizi kwa nabii huyo ataangamizwa kabisa atoke kati ya watu.' 24 Ndiyo,
na manabii wote tokea Samweli na wale waliofuata baada yake, walizungumza na
walitangaza siku hizi. 25 Ninyi ni wana wa manabii na wa agano ambalo Mungu
alilifanya pamoja na mababu, kama alivyosema kwa Abrahamu, 'Katika mbegu
yako familia zote za dunia zitabarikiwa.' 26 Baada ya Mungu kumwinua mtumishi
wake, alimtuma kwenu kwanza, ili awabariki ninyi kwa kugeuka kutoka katika uovu
wenu.”

# 4

1 Wakati Petro na Yohana walipokuwa wakizungumza na watu, makuhani na
mlinzi wa hekalu na masadukayo waliwaendea. 2 Walikuwa wameudhika sana
kwa sababu Petro na Yohana walikuwa wanawafundisha watu kuhusu Yesu na
kutangaza juu ya kufufuka kwake kutoka kwa wafu. 3 Waliwakamata na kuwaweka
gerezani hadi asubuhi iliyofuata, kwani tayari ilikuwa jioni. 4 Lakini watu
wengi waliokuwa wamesikia ujumbe waliamini; na idadi ya wanaume waliokuwa
wameamini walikadiliwa kuwa elfu tano. 5 Hata ilipofika asubuhi siku iliyofuata,
kwamba wakuu wao, wazee na waandishi, kwa pamoja walikusanyika Yerusalemu.
6 Anasi kuhani mkuu alikuwepo, na Kayafa, na Yohana, na Iskanda, na wote
waliokuwa ni ndugu wa kuhani mkuu. 7 Walipokuwa wamewaweka Petro na Yohana
katikati yao, waliwauliza, “Kwa uwezo gani, au kwa jina gani mmefanya hili?”
8 Kisha, Petro, akiwa amejaa Roho Mtakatifu, akawaambia, “Ninyi wakuu wa watu, na
wazee, 9 kama sisi siku ya leo tunahojiwa kuhusu tendo jema lililofanywa kwa mtu
huyu mgonjwa - kwa namna gani mtu huyu alifanywa mzima? 10 Hebu lijulikane
hilo kwenu na kwa watu wote katika Israel, kwamba kwa jina la Yesu Kristo wa
Nazareti, ambaye mlimsulibisha, ambaye Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, ni
kwa njia yake kwamba mtu huyu anasimama hapa mbele yenu akiwa mwenye afya.
11 Yesu Kristo ni jiwe ambalo ninyi wajenzi mlilidharau, lakini ambalo limefanywa
kuwa jiwe kuu la pembeni. 12 Hakuna wokovu katika mtu mwingine awaye yote.
Kwa maana hakuna jina jingine chini ya mbingu walilopewa watu, ambalo kwa hilo
tunaweza kuokolewa.” 13 Sasa walipoona ujasiri wa Petro na Yohana, na wakagundua
kwamba walikuwa ni watu wakawaida wasio na elimu, walishangaa, wakafahamu
kwamba Petro na Yohana wamekuwa pamoja na Yesu. 14 Kwa sababu walimwona
yule mtu aliyeponywa amesimama pamoja nao, hawakuwa na kitu cha kusema dhidi
ya hili. 15 Lakini walipokuwa wamekwisha kuwaamuru mitume waondoke mbele ya
mkutano wa baraza, walizungumza wao kwa wao. 16 Walisema, tutawafanyaje watu
hawa? Ni kweli kwamba muujiza wa ajabu umefanyika kupitia wao unajulikana na
kila mmoja anayeishi Yerusalemu; hatuwezi kulikataa hilo. 17 Lakini, ili kwamba
jambo hili lisienee miongoni mwa watu, hebu tuwaonye wasinene tena kwa mtu
yeyote kwa jina hili. 18 Waliwaita Petro na Yohana ndani na kuwaamuru kamwe
wasinene wala kufundisha kwa jina la Yesu. 19 Lakini Petro na Yohana walijibu
na kuwaambia, “Kama ni sahihi machoni pa Mungu kuwatii ninyi kuliko Mungu,
hukumuni wenyewe. 20 Maana sisi hatuwezi kuacha kuyanena mambo ambayo

tumeyaona na kuyasikia.” 21 Baada ya kuwaonya sana Petro na Yohana, waliwaacha
waende. Hawakuweza kupata sababu yoyote ya kuwaadhibu, kwa sababu watu wote
walikuwa wakimsifu Mungu kwa kile kilichokuwa kimetendeka. 22 Mtu aliyekuwa
amepokea muujiza wa uponyaji alipata kuwa na umri zaidi ya miaka arobaini.
23 Baada ya kuwaacha huru, Petro na Yohana walikuja kwa watu wao na kuwataarifu
yote ambayo makuhani wakuu na wazee walikuwa wamewaambia. 24 Walipoyasikia,
walipaza sauti zao kwa pamoja kwa Mungu na kusema, “Bwana, wewe uliyeumba
mbingu na dunia na bahari na kila kitu ndani yake, 25 wewe ambaye, kwa Roho
Mtakatifu, kwa kinywa cha baba yetu Daudi, mtumishi wako, ulisema, “Kwanini watu
wa mataifa wamefanya ghasia, na watu wametafakari mambo yasiyofaa? 26 Wafalme
wa dunia wamejipanga pamoja, na watawala wamekusanyika kwa pamoja dhidi ya
Bwana na dhidi ya masihi wake.” 27 Ni hakika, wote Herode na Pontio Pilato, pamoja
na watu wa mataifa na watu wa Israeli, walikusanyika kwa pamoja katika mji huu
dhidi ya mtumishi wako mtakatifu Yesu, ambaye ulimpaka mafuta. 28 Walikusanyika
kwa pamoja kufanya yote ambayo mkono wako na mapenzi yako yaliyaamuru tangu
awali kabla hayajatokea. 29 Sasa, Bwana, yaangalie matisho yao, na ukawajaalie
watumishi wako kulinena neno lako kwa ujasiri wote. Ili 30 kwamba unaponyosha
mkono wako kuponya, ishara na maajabu viweze kutokea kupitia jina la mtumishi
wako mtakatifu Yesu.” 31 Walipomaliza kuomba, eneo ambalo walikusanyika kwa
pamoja likatikiswa, na wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, na walinena neno la
Mungu kwa ujasili. 32 Idadi kubwa ya wale walioamini walikuwa na moyo mmoja
na roho moja: na hakuna hata mmoja wao aliyesema kwamba chochote alichomiliki
kilikuwa cha kwake mwenyewe; badala yake walikuwa na vitu vyote shirika. 33 Kwa
nguvu kubwa mitume walikuwa wakiutangaza ushuhuda wao kuhusu ufufuo wa
Bwana Yesu, na neema kubwa ilikuwa juu yao wote. 34 Hapakuwa na mtu yeyote
miongoni mwao aliyepungukiwa na mahitaji, kwa sababu watu wote waliokuwa na
hati za viwanja au nyumba, waliviuza na kuleta pesa ya vitu waliyokuwa wameuza
35 na kuviweka chini ya miguu ya mitume. Na mgawanyo ulifanywa kwa kila
muumini, kulingana na kila mmoja alivyokuwa na hitaji. 36 Yusufu, mlawi, mtu
kutoka Kipro, alipewa jina la Barnabasi na mitume (hiyo ikitafasiriwa, ni mwana
wa faraja). 37 Akiwa na shamba, aliliuza na akaleta fedha, akaziweka chini ya miguu
ya mitume.

# 5

1 Hivyo, mtu mmoja aliyeitwa Anania, na Safira mkewe, waliuza sehemu ya mali,
2 na akaficha sehemu ya fedha waliyouza (mke wake pia alilijua hili), na akaleta
sehemu iliyobakia na kuiweka kwenye miguu ya mitume. 3 Lakini Petro akasema,
“Anania, kwa nini shetani ameujaza moyo wako kusema uongo kwa Roho Mtakatifu
na kuficha sehemu ya mali ya shamba? 4 Wakati lilipokuwa halijauzwa, halikuwa ni
mali yako? Na baada ya kuuzwa, halikuwa chini ya uamuzi wako? Ilikuwaje uwaze
jambo hili moyoni mwako? Hujawadanganya wanadamu, bali umemdanganya
Mungu.” 5 Katika kusikia maneno haya, Anania alidondoka chini na akakata roho.
Na hofu kubwa iliwajia wote waliolisikia hili. 6 Vijana wakaja mbele na kumtia
katika sanda, na kumpeleka nje na kumzika. 7 Baada ya masaa matatu hivi, mke
wake aliingia ndani, asijue ni nini kilichokuwa kimetokea. 8 Petro akamwambia,
“Niambie, kama mliuza shamba kwa thamani hiyo.” Akasema, “Ndiyo, kwa thamani
hiyo.” 9 Kisha Petro akamwambia, “Inakuwaje kwamba mmepatana kwa pamoja
kumjaribu Roho wa Bwana? Angalia, miguu ya wale waliomzika mme wako iko
mlangoni, na watakubeba na kukupeleka nje.” 10 Ghafla akadondoka miguuni
pa Petro, akakata roho, na wale vijana wakaja ndani wakamkuta ameshakufa.

Wakambeba kumpeleka nje, na kumzika karibu na mmewe. 11 Hofu kubwa ikaja
juu ya kanisa zima, na juu ya wote walioyasikia mambo haya. 12 Ishara nyingi
na maajabu vilikuwa vinatokea miongoni mwa watu kupitia mikono ya mitume.
Walikuwa pamoja katika ukumbi wa Sulemani. 13 Lakini, hakuna mtu mwingine
tofauti aliyekuwa na ujasiri wa kuambatana nao; hata hivyo, walipewa heshima ya
juu na watu. 14 Na pia, waamini wengi walikuwa wakiongezeka kwa Bwana, idadi
kubwa ya wanaume na wanawake, 15 kiasi kwamba hata waliwabeba wagonjwa
mitaani, na kuwalaza vitandani na kwenye makochi, ili kwamba Petro akiwa anapita,
kivuli chake kiweze kushuka juu yao. 16 Hapo pia, idadi kubwa ya watu walikuja
kutoka miji iliyozunguka Yerusalem, wakiwaleta wagonjwa na wote waliopagawa
na roho wachafu, na wote waliponywa. 17 Lakini kuhani mkuu aliinuka, na wote
waliokuwa pamoja naye (ambao ni wa dhehebu la masadukayo); na walijawa na
wivu 18 wakanyosha mikono yao kuwakamata mitume na kuwaweka ndani ya gereza
la jumla. 19 Na wakati wa usiku malaika wa Bwana akaifungua milango ya gereza
na kuwaongoza nje na kusema, 20 "Nendeni, mkasimame hekaluni na kuwaambia
watu maneno yote ya Uzima huu." 21 Waliposikia hili, waliingia hekaluni wakati wa
kupambazuka na kufundisha. Lakini, kuhani mkuu alikuja na wote waliokuwa naye,
na kuitisha baraza lote kwa pamoja, na wazee wote wa watu wa Israeli, na kuwatuma
gerezani ili kuwaleta mitume. 22 Lakini watumishi waliokwenda, hawakuwakuta
gerezani, walirudi na kutoa taarifa, 23 "Tumekuta gereza limefungwa vizuri salama,
na walinzi wamesimama langoni, lakini tulipokuwa tukifungua, hatukuona mtu
ndani." 24 Sasa wakati jemedari wa hekalu na makuhani wakuu waliposikia maneno
haya, waliingiwa na shaka kubwa kwa ajili yao wakiwaza litakuwaje jambo hili.
25 Kisha mmoja akaja na kuwaambia, "Watu mliowaweka gerezani wamesimama
hekaluni na wanafundisha watu." 26 Hivyo jemedari alienda pamoja na watumishi,
na wakawaleta, lakini bila ya kufanya vurugu, kwa sababu waliwaogopa watu
wangeweza kuwapiga kwa mawe. 27 Walipokwisha kuwaleta, waliwaweka mbele
ya baraza. Kuhani mkuu aliwahoji 28 akisema, "Tuliwaamuru msifundishe kwa jina
hili, na bado mmeijaza Yerusalemu kwa fundisho lenu, na kutamani kuleta damu
ya mtu huyu juu yetu." 29 Lakini Petro na mitume wakajibu, "Lazima tumtii Mungu
kuliko watu. 30 Mungu wa baba zetu alimfufua Yesu, mliyemuua, kwa kumtundika
juu ya mti. 31 Mungu alimtukuza katika mkono wake wa kuume, na kumfanya
kuwa Mkuu na mwokozi, kutoa toba kwa Israeli, na msamaha wa dhambi. 32 Sisi ni
mashahidi wa mambo haya, na Roho Mtakatifu, ambaye Mungu amemtoa kwa wale
wanaomtii." 33 Wajumbe wa baraza waliposikia hivi, walishikwa na hasira wakataka
kuwaua mitume. 34 Lakini pharisayo aliyeitwa Gamalieli, mwalimu wa sheria,
aliyeheshimiwa na watu wote, alisimama na kuwaamuru mitume wachukuliwe
nje kwa muda mfupi. 35 Kisha akawaambia, "Wanaume wa Israeli, iweni makini
sana na kile mnachopendekeza kuwafanyia watu hawa. 36 Kwa sababu, zamani
zilizopita, Theuda aliinuka na kujidai kuwa mtu mkuu, na idadi ya watu, wapata
mia nne walimfuata. Aliuawa, na wote waliokuwa wanamtii walitawanyika na
kupotea. 37 Baada ya mtu huyu, Yuda mgalilaya, aliinuka siku zile za kuandikwa
sensa, akavuta watu wengi nyuma yake. Naye pia alipotea na wote waliokuwa
wakimtii walitawanyika. 38 Sasa nawaambia, jiepusheni na watu hawa na muwaache
wenyewe, kwa sababu, kama mpango huu au kazi hii ni ya watu itatupwa. 39 Lakini
kama ni ya Mungu, hamtaweza kuwazuia; mnaweza mkajikuta hata mnashindana
na Mungu." Hivyo, walishawishika na maneno yake. 40 Kisha, waliwaita mitume
ndani na kuwachapa na kuwaamuru wasinene kwa jina la Yesu, na wakawaacha
waende zao. 41 Waliondoka mbele ya baraza wakifurahi kwa sababu wamehesabiwa
kuwa wamestahili kuteseka na kutoheshimiwa kwa ajili ya Jina hilo. 42 Kwa hiyo,

kila siku, ndani ya hekalu na kutoka nyumba hadi nyumba waliendelea kufundisha
na kuhubiri Yesu kuwa ni Masihi.

## 6

1 Sasa katika siku hizi, wakati idadi ya wanafunzi ilipokuwa inaongezeka, lalamiko
la Wayahudi wa Kiyunani lilianza dhidi ya Waebrania, kwa sababu wajane wao
walikuwa wanasahaulika katika mgao wa kila siku wa chakula. 2 Mitume kumi na
wawili waliwaita kusanyiko lote la wanafunzi na kusema, “Siyo sahihi kwetu kuliacha
neno la Mungu na kuhudumia mezani. 3 Kwa hiyo, ndugu, chagueni, wanaume saba,
kutoka miongoni mwenu, watu wema, waliojaa Roho na hekima, ambao tunaweza
kuwakabidhi huduma hii. 4 Na sisi, tutaendelea daima katika kuomba na katika
huduma ya neno.” 5 Hotuba yao ikaupendeza mkutano wote. Hivyo, wakamchagua
Stefano, mtu aliyejaa imani na Roho Mtakatifu, na Filipo, Prokoro, Nikanori, Timoni,
Parmena, na Nikolao, mwongofu kutoka Antiokia. 6 Waumini waliwaleta watu hawa
mbele ya mitume, walioomba na badaye wakawawekea mikono yao. 7 Hivyo, neno la
Mungu lilienea; na idadi ya wanafunzi ilizidi kuongezeka huko Yesrusalem; na idadi
kubwa ya makuhani wakaitii imani. 8 Na Stefano, aliyejaa neema na nguvu, alikuwa
akifanya maajabu na ishara kubwa miongoni mwa watu. 9 Lakini hapo wakainuka
baadhi ya watu wafuasi wa Sinagogi liitwalo Sinagogi la Mahuru, na la Wakirene na la
Waeskanderia, na baadhi kutoka Kilikia na Asia. Watu hawa walikuwa wakihojiana
na Stefano. 10 Lakini, hawakuweza kushindana na hekima na Roho ambayo Stefano
alikuwa akitumia katika kuzungumza. 11 Kisha waliwashawishi baadhi ya watu kwa
siri kusema, “Tumesikia Stefano akizungumza maneno ya kufuru dhidi ya Musa na
dhidi ya Mungu.” 12 Waliwashurutisha watu, wazee, na waandishi, na kumwendea
Stefano, wakamkamata, na kumleta mbele ya baraza. 13 waliwaleta mashahidi wa
uongo, waliosema, “mtu huyu haachi kunena maneno mabaya dhidi ya eneo hili
takatifu na sheria. 14 Kwani tumemsikia akisema kwamba huyu Yesu wa Nazareti
atapaharibu mahali hapa na kuzibadili desturi tulizokabidhiwa na Musa.” 15 Kila
mmoja aliyekuwa katika baraza, akaelekeza macho yake kumwangalia Stefano, nao
wakauona uso wake ulikuwa kama uso wa malaika.

## 7

1 Kuhani mkuu akasema,”mambo haya ni ya kweli”? 2 Stephano akasema, “Ndugu
na mababa zangu, nisikilizeni mimi: Mungu wa utukufu alimtokea baba yetu
Abrahamu wakati alipokuwa Mesopotamia, kabla hajaishi Harani,' 3 akamwambia,'
Ondoka katika nchi yako na jamaa zako na uende katika nchi nitakayokuonyesha'.
4 Kisha akaondoka katika nchi ya Ukaldayo akaishi Harani, kutoka hapo, baada ya
baba yake kufa, Mungu akamleta kwenye nchi hii, wanayoishi sasa. 5 Hakumpa
chochote kama urithi wake, hapakuwa na sehemu hata ya kuweka mguu. Lakini
Abrahamu aliahidiwa hata kabla hajapata mtoto kuwa atapewa nchi kama miliki
yake na uzao wake. 6 Mungu alinena naye hivi, ya kwamba wazao wake wangeishi
katika nchi ya ugeni, na kwamba wenyeji wa huko watawafanya kuwa watumwa
wao na kuwatenda vibaya kwa muda wa miaka mia nne. 7 Na Mungu akasema,
nitalihukumu taifa ambalo litawafanya mateka, na baada ya hapo watatoka na
kuniabudu katika sehemu hii.' 8 Na akampa Abrahamu agano la tohara, hivyo
Abrahamu akawa baba wa Isaka akamtahiri siku ya nane; Isaka akawa baba wa
Yakobo, na Yakobo akawa baba wa mababu zetu kumi na wawili. 9 Mababu zetu
wakamwonea wivu Yusufu wakamuuza katika nchi ya Misri, na Mungu alikuwa
pamoja naye, 10 na akamwokoa katika mateso yake, na akampa fadhili na hekima
mbele ya Farao mfalme wa Misri. Farao akamfanya awe mtawala juu ya Misri
na juu ya nyumba yake yote. 11 Basi kukawa na njaa kuu na mateso mengi

katika nchi ya Misri na Kanani, na baba zetu hawakupata chakula. 12 Lakini
Yakobo aliposikia kuna nafaka Misri, aliwatuma baba zetu kwa mara ya kwanza.
13 Katika safari ya pili Yusufu akajionyesha kwa ndugu zake, familia ya Yusufu
ikajulikana kwa Farao. 14 Yusufu akawatuma ndugu zake kwenda kumwambia
Yakobo baba yao aje Misri, pamoja na jamaa yake, jumla ya watu wote ni sabini
na tano. 15 Hivyo Yakobo akashuka Misri; kisha akafa yeye pamoja na baba
zetu. 16 Wakachukuliwa hata Shekemu wakazikwa katika kaburi ambalo Abrahamu
alilinunua kwa vipande vya fedha kutoka kwa wana wa Hamori huko Shekemu.
17 Wakati wa ile ahadi ambayo Mungu alimwahidi Abrahamu ulipokaribia, watu
wakiwa wameongezeka huko Misri, 18 wakati huo aliinuka mfalme mwingine juu ya
Misri, mfalme asiyejua kuhusu Yusufu. 19 Huyo mfalme mwingine akawadanganya
watu wetu na kuwatenda mabaya baba zetu, na kuwatupa watoto wao wachanga
ili wasiishi. 20 Katika kipindi kile Musa alizaliwa; alikuwa mzuri mbele za Mungu,
akalelewa miezi mitatu katika nyumba ya baba yake. 21 Wakati alipotupwa, binti
wa Farao alimchukua akamlea kama mwanaye. 22 Musa alifundishwa mafundisho
yote ya Kimisri; alikuwa na nguvu katika maneno na matendo. 23 Lakini baada ya
kutimiza miaka arobaini, ikamjia katika moyo wake kuwatembelea ndugu zake, wana
wa Israeli. 24 Alipomwona Mwisraeli akitendewa mabaya, Musa alimtetea na kulipiza
kisasi aliyekuwa akimwonea kwa kumpiga Mmisiri: 25 akifikiri kuwa ndugu zake
watafahamu kwamba Mungu anawaokoa kwa mkono wake, lakini hawakufahamu.
26 Siku iliyofuata akaenda kwa baadhi ya Waisraeli waliokuwa wanagombana;
akajaribu kuwapatanisha; akisema,' Mabwana, Ninyi ni ndugu; mbona mnakoseana
ninyi kwa ninyi,? 27 Lakini aliyemkosea jirani yake akamsukumia mbali, na kusema,
'Nani kakufanya mtawala na muhukumu wetu? 28 Wewe unataka kuniua, kama
ulivyomuua Mmisri jana?” 29 Musa akakimbia baada ya kusikia hivyo; akawa mgeni
katika nchi ya Midiani, ambapo akawa baba wa wana wawili. 30 Baada ya miaka
arobaini kupita, malaika akamtokea katika jangwa la mlima Sinai, katika mwali wa
moto ndani ya kichaka. 31 Wakati Musa alipoona moto, alishangaa na kustaajabia
kile alichokiona, na alipojaribu kukisogelea ili kukitazama, sauti ya Bwana ikamjia
Ikisema, 32 'Mimi ni Mungu wa baba zako, Mungu wa Abrahamu, na wa Isaka, na
wa Yakobo'. Musa alitetemeka na hakuthubutu kuangalia. 33 Bwana akamwambia,
'Vua viatu vyako, sehemu uliposimama ni mahali patakatifu. 34 Nimeona mateso ya
watu wangu waliopo Misri; Nimesikia kuugua kwao, nami nimeshuka ili niwaokoe;
sasa njoo, nitakutuma wewe Misri.' 35 Huyu Musa ambaye waliyemkataa, wakati
waliposema, 'nani kakufanya kuwa mtawala na mwamuzi wetu?'_ alikuwa ndiye
ambaye Mungu alimtuma awe mtawala na mkombozi. Mungu alimtuma kwa mkono
wa malaika ambaye alimtokea Musa kichakani. 36 Musa aliwaongoza kutoka Misri
baada ya kufanya miujiza na ishara katika Misri na katika bahari ya Shamu, na
katika jangwa kwa kipindi cha miaka arobaini. 37 Ni Musa huyu ndiye aliyewambia
watu wa Isiraeli kuwa, 'Mungu atawainulieni nabii kutoka miongoni mwa ndugu
zenu, nabii kama mimi'. 38 Huyu ni mtu ambaye alikuwa katika mkutano jangwani
na malaika ambaye aliongea naye katika mlima Sinai. Huyu ndiye mtu ambaye
alikuwa na baba zetu, huyu ni mtu ambaye alipokea neno lililo hai na kutupatia
sisi. 39 Huyu ni mtu ambaye baba zetu walikataa kumtii; walimsukumia mbali,
na katika mioyo yao waligeukia Misri. 40 Katika kipindi hicho walimwambia
Haruni.'tutengenezee miungu itakayotuongoza. Huyo Musa, aliyekuwa akituongoza
kutoka katika nchi ya Misri, hatujui kilichompata.' 41 Hivyo wakatengeneza ndama
kwa siku hizo na wakatoa sadaka kwa hiyo sananmu na wakafurahi kwa sababu
ya kazi ya mikono yao. 42 Lakini Mungu aliwageuza na kuwapa waabudu nyota
wa angani, kama ilivyoandikwa kwenye kitabu cha manabii, 'Je Mmenitolea mimi

sadaka za wanyama mliowachinja jangwani kwa muda wa miaka arobaini, nyumba
ya Israeli? 43 Mmekubali hema ya kukutania ya Moleki na nyota ya mungu refani,
na picha mliyoitengeneza na kuwaabudu wao: na nitawapeleka mbali zaidi ya
Babeli.' 44 Baba zetu walikuwa na hema ya kukutania ya ushuhuda jangwani, kama
Mungu alivyoamuru alipoongea na Musa, kwamba angeitengeneza kwa mfano wa ule
aliouona. 45 Hili ni hema ambalo baba zetu, kwa wakati wao, walileta katika nchi
na Joshua. Hii ilitokea wakati walipoingia kumiliki taifa ambalo Mungu aliwafukuza
kabla ya uwepo wa baba zetu. Hii ilikuwa hivi hadi siku za Daudi, 46 ambaye
alipata kibali machoni pa Mungu,' na akaomba kutafuta makao kwa Mungu wa
Yakobo. 47 Lakini Selemani alimjengea nyumba ya Mungu. 48 Hata hivyo Aliye Juu
haishi kwenye nyumba zilizojengwa kwa mikono; hii ni kama nabii alivyosema,
49 Mbingu ni kiti changu cha enzi, na dunia ni sehemu ya kuwekea miguu yangu.
Nyumba ya aina gani mtanijengea?, asema Bwana: au ni wapi sehemu yangu
ya kupumzikia? 50 Siyo mkono wangu uliofanya hivi vitu vyote?' 51 Enyi watu
wenye shingo ngumu msiotahiriwa mioyo na masikio, kila mara mnampinga Roho
Mtakatifu,' mnatenda kama baba zenu walivyotenda. 52 Ni nabii gani katika manabii
ambaye baba zenu hawakumtesa?. Waliwaua manabii wote waliotokea kabla ya ujio
wa Mmoja mwenye Haki,'na sasa mmekuwa wasaliti na wauaji wake pia, 53 enyi
watu mliopokea sheria ile iliyoagizwa na malaika lakini hamkuishika." 54 Kisha
wajumbe wa baraza waliposikia mambo haya, walichomwa mioyo yao, wakamsagia
meno Stefano. 55 Lakini yeye, akiwa amejaa Roho Mtakatifu, alitazama mbinguni
kwa makini na akauona utukufu wa Mungu,' na kumwona Yesu amesimama mkono
wa kuume wa Mungu. 56 Stefano akasema, "Angalia nimeona mbingu zimefunguka,
na Mwana wa Adam amesimama mkono wa kuume wa Mungu." 57 Lakini wajumbe
wa baraza wakapiga kelele kwa sauti za juu, wakaziba masikio yao, wakamkimbilia
kwa pamoja, 58 wakamtupa nje ya mji na wakampiga mawe: na mashahidi wakavua
nguo zao za nje na kuweka chini karibu na miguu ya kijana aliyeitwa Sauli.
59 Walipokuwa wakimpiga mawe Stefano, aliendelea kumwita Bwana na kusema,
"Bwana Yesu, pokea roho yangu,". 60 Akapiga magoti na kuita kwa sauti kubwa,
"Bwana, usiwahesabie dhambi hii. "Aliposema haya, akakata roho.

# 8

1 Sauli alikuwa kwenye makubaliano ya kifo chake. siku hiyo ndipo
alipoanza kuwatesa kinyume cha kanisa lililokuwa Yerusalemu; na waaminio
wote waliotawanyika katika majimbo ya Yudea na Samaria, isipokuwa mitume.
2 Watu wachamungu walimzika Stefano na kufanya maombolezo makubwa juu
yake. 3 Lakini Sauli alililidhuru sana kanisa. Alikwenda nyumba kwa nyumba na
kuwaburuza nje wanawake na waume, na kuwatupia gerezani. 4 waaminio ambao
walikuwa wametawanyika bado walilihubiri neno. 5 Filipo akashuka katika mji
wa Samaria na akamtangaza Kristo huko. 6 Baada ya makutano kusikia na kuona
ishara alizofanya Filipo; wakaweka umakini juu ya kile alichosema. 7 Kutoka hapo
watu wengi waliosikia, pepo wachafu waliwatoka watu huku wakilia kwa sauti
kubwa, na wengi waliopooza na viwete waliponywa. 8 Na kulikuwa na furaha
kubwa katika mji. 9 Lakini palikuwa na mtu mmoja katika mji ule jina lake Simon,
ambaye alikuwa akifanya uchawi; ambao aliutumia kuwashangaza watu wa taifa la
Samaria, wakati akisema kuwa yeye ni mtu wa muhimu. 10 Wasamaria wote tangu
mdogo hata mkubwa, wakamsikiliza; wakasema;"mtu huyu ni ile nguvu ya Mungu
ambayo ni kuu." 11 Wakamsikiliza, kwa maana amewashangaza muda mrefu kwa
uchawi wake. 12 Lakini wakati walipoamini kuwa Filipo alihubiri juu ya ufalme
wa Mungu na juu ya jina la Yesu Kristo, walibatizwa, wanaume kwa wanawake.

13 Na Simoni mwenyewe aliamini: baada ya kubatizwa, aliendelea kuwa na Filipo;
alipoona ishara na miujiza iliyokuwa ikitendeka, alishangaa. 14 Wakati mitume wa
Yerusalemu waliposikia kuwa Samaria imepokea neno la Mungu, wakawatuma Petro
na Yohana. 15 Wakati walipokuwa wakishuka wakawaombea; kwamba wampokee
Roho Mtakatifu. 16 Mpaka muda huo, Roho Mtakatifu alikuwa hajawashukia hata
mmoja wao; walikuwa tu wamebatizwa kwa jina la Bwana Yesu. 17 Ndipo Petro na
Yohana wakawawekea mikono, nao wakampokea Roho Mtakatifu. 18 Wakati Simoni
alipoona kwamba Roho Mtakatifu ametolewa kupitia kuwekewa mikono na mitume;
akataka kuwapa pesa, 19 Akasema, “Nipeni hii nguvu, ili kila nitakayemwekea mikono
apokee Roho Mtakatifu.” 20 Lakini Petro akamwambia; pesa yako pamoja na wewe
ipotelee mbali, kwa sababu umedhani kuwa karama ya Mungu inapatikana kwa pesa.
21 Hauna sehemu katika jambo hili, kwa sababu moyo wako si mnyoofu mbele za
Mungu. 22 Hivyo basi tubu maovu yako na kumwomba Mungu labda utasamehewe
fikra za moyo wako. 23 Kwa maana naona uko katika sumu ya uchungu na kifungo
cha dhambi.” 24 Simoni akajibu na kusema, “Mwombeni Bwana kwa ajili yangu, kwa
kuwa mambo yote mliyozungumza yaweza kunitokea. 25 Wakati Petro na Yohana
walipokuwa wameshuhudia na kuhubiri neno la Bwana, walirudi Yerusalemu kwa
njia hiyo; walihubiri injili katika vijiji vingi vya Wasamaria. 26 Basi malaika wa
Bwana akanena na Filipo na kusema, “Angaza na uende kusini katika njia iendayo
chini ya Yerusalemu kuelekea Gaza.” ( Njia hii iko katika jangwa). 27 Akaangaza
na kwenda. Tazama, kulikuwa na mtu wa Ethiopia, towashi mwenye mamlaka
kuu chini ya kandase; malkia wa Ethiopia. Aliyewekwa juu ya hazina yake yote;
naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu. 28 Alikuwa akirejea ameketi garini
mwake akisoma chuo cha nabii Isaya. 29 Roho akasema na Filipo, “Sogea karibu
na gari hili ukashikamane nalo. 30 “Hivyo Filipo akaenda mbio, akamsikia akisoma
katika chuo cha nabii Isaya; akasema, Je unafahamu unachosoma?” 31 Muethiopia
akasema, “nitawezaje mtu asiponiongoza?” Akamsihi Filipo apande garini na
kuketi pamoja naye. 32 Sasa fungu la maandiko alilokuwa akisoma Muethiopia ni
hili; Aliongozwa kama kondoo kwenda machinjioni kuchinjwa; na kama kondoo
alinyamaza kimya, hakufungua kinywa chake: 33 Kwa kuhuzunishwa kwake hukumu
yake iliondolewa: Nani ataeleza kizazi chake? maisha yake yameondolewa katika
nchi.” 34 Hivyo towashi akamwuliza Filipo, na kusema, “nakuomba, ni nabii
yupi ambaye anaongelewa habari zake, ni kuhusu yeye, au za mtu mwingine”?.
35 Filipo alianza kuongea, alianza kwa andiko hili la Isaya kumhubiria habari za
Yesu. 36 Wakiwa njiani, wakafika penye maji,' towashi akasema, “Tazama, pana
maji hapa nini kinazuia nisibatizwe?, 37 maneno haya, “Hivyo Muethiopia akajibu
“naamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu,” hayamo kwenyemaandiko ya
kale). Ndipo Muethiopia akaamuru gari lisimame. 38 Walikwenda ndani ya maji,
pamoja Filipo na towashi, Filipo akambatiza. 39 Wakati walipotoka kwenye maji,
Roho wa Bwana ikampeleka Filipo mbali; towashi hakumwona, akaenda njia yake
akishangilia. 40 Lakini Philipo akatokea Azoto. Alipita katika mkoa ule na kuhubiri
injili katika miji yote mpaka alipofika Kaisaria.

# 9

1 Lakini Sauli, aliendelea kusema vitisho hata vya kifo kwa wanafunzi wa Bwana,
alikwenda kwa kuhani mkuu 2 na kumwomba barua kwa ajili ya masinagogi
huko Dameski, ili kwamba akimpata mtu aliye katika Njia ile, awe mwanaume au
mwanamke, awafunge na kuwaleta Yerusalemu. 3 Hata alipokuwa akisafiri, ilitokea
kwamba alipokaribia Dameski, ghafla ikamwangaza kotekote nuru kutoka mbinguni,'
4 naye akaanguka chini na akasikia sauti ikimwambia,”Sauli, Sauli, mbona wanitesa

mimi?” 5 Sauli akajibu, U nani wewe Bwana? Bwana akasema, “ Mimi ndiye
Yesu unayeniudhi; 6 Lakini inuka, ingia mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda
7 Wale watu waliosafiri pamoja na Sauli wakatulia kimya, wakisikiliza sauti, wasione
mtu. 8 Sauli akainuka katika nchi na alipofungua macho yake, hakuweza kuona kitu,
wakamshika mkono wakamleta mpaka Dameski. 9 Kwa siku tatu haoni, hali, wala
hanywi. 10 Basi palikuwapo mwanafunzi Dameski jina lake Anania, Bwana alisema
naye katika maono, “Anania.” Na akasema, “Tazama, nipo hapa, Bwana. 11 “Bwana
akamwambia, “Inuka uenda zako katika mtaa uitwao Nyofu, na katika nyumba ya
Yuda na ukaulize mtu kutoka Tarso aitwaye Sauli; maana angali anaomba; 12 na
alimwona katika maono mtu jina lake Anania akiingia na kumwekea mikono juu
yake ili kwamba apate kuona. 13 Lakini Anania akajibu, “Bwana, nimesikia habari
za mtu huyu kwa watu wengi, kwa kiasi gani alivyowatendea mabaya watakatifu wa
huko Yerusalemu; 14 Hapa ana mamlaka kutoka kwa kuhani mkuu kumkamata kila
mmoja anayeliitia jina lako. 15 Lakini Bwana akamwambia, “Nenda, kwa maana yeye
ni chombo teule kwangu, alichukue jina langu mbele ya Mataifa na wafalme na wana
wa Israeli. 16 Maana nitawaonesha yalivyo mengi yatakayompasa kuteswa kwa ajili
ya jina langu”. 17 Anania akaenda, akaingia mle nyumbani; Akamwekea mikono
akasema, Ndugu Sauli, Bwana Yesu, aliyekutokea katika njia ulipokuwa unakuja,
amenituma upate kuona tena na ujazwe Roho Mtakatifu. 18 Ghafla vikaanguka
machoni pake vitu kama magamba, akapata kuona, akasimama, akabatizwa; akala
chakula na kupata nguvu. 19 Akakaa pamoja na wanafunzi huko Dameski kwa
siku nyingi. 20 Wakati huo huo akamtangaza Yesu katika masinagogi, akisema
kwamba yeye ni Mwana wa Mungu. 21 Na wote waliosikia walishangaa na kusema,
“Siyo mtu huyu aliyewaharibu wote walioita Jina hili huko Yerusalemu? Na hapa
alikuja kwa kusudi la kuwafunga na kuwapeleka kwa makuhani.” 22 Lakini Sauli
aliwezeshwa kuhubiri na kuwafanya Wayahudi waliokaa Dameski wachanganyikiwe
na kuthibitisha ya kuwa huyu ndiye Kristo. 23 Baada ya siku nyingi, Wayahudi
wakafanya shauri pamoja ili wamuue. 24 Lakini mpango wao ukajulikana na Sauli.
Wakamvizia mlangoni mchana na usiku wapate kumuua. 25 Lakini wanafunzi wake
wakamchukua usiku wakamshusha kupitia ukutani, wakamtelemsha chini katika
kapu. 26 Na Sauli alipofika Yerusalemu, alijaribu kujiunga na wanafunzi lakini
walikuwa wakimuogopa, wasisadiki kuwa yeye ni mwanafunzi. 27 Lakini Barnaba
akamchukua na kumpeleka kwa mitume, Na akawaeleza jinsi Sauli alivyomuona
Bwana njiani na Bwana alivyosema nae, na jinsi Sauli alivyohubiri kwa ujasiri kwa
jina la Yesu huko Dameski. 28 Alikutana nao walipoingia na kutoka Yerusalemu.
Akanena kwa ujasiri kwa jina la Bwana Yesu, 29 akihojiana na Wayahudi wa Kiyunani
lakini wakijaribu mara kwa mara kumuua. 30 Wakati ndugu walipojua jambo
hilo, wakamchukua mpaka Kaisaria, na wampeleke aende Tarso. 31 Basi kanisa
lote katika Uyahudi, Galilaya na Samaria, lilikuwa na amani, na likajengwa, na
kutembea katika hofu ya Bwana na faraja ya Roho Mtakatifu, kanisa likakua kwa
kuongezeka idadi. 32 Kisha ilitokea Petro alipokuwa akizungukazunguka pande zote
za mkoa, akawateremkia waumini waishio katika mji wa Lida. 33 Akamuona huko
mtu mmoja jina lake Ainea, mtu huyo amekuwa kitandani miaka minane; maana
alikuwa amepooza. 34 Petro akamwambia, “Ainea, Yesu Kristo akuponye; Amka
na ujitandikia kitanda chako,” Mara akaamka. 35 Na watu wote waliokaa Lida na
Sharoni walipomuona mtu huyo, walimgeukia Bwana. 36 Palikuwa na mwanafunzi
Yafa aitwaye Tabitha, ambalo lilitafsiriwa kama “Dorcas” Huyu mwanamke alijaa
kazi njema na matendo ya rehema aliyoyafanya kwa maskini. 37 Ilitokea katika
siku hizo aliugua na akafa; walipomsafisha, walimpandisha chumba cha juu na

kumlaza.. 38 Kwa vile Lida ilikuwa karibu na Yafa, na wanafunzi walisikia kwamba
Petro alikuwa huko, waliwatuma watu wawili kwake, wakimsihi, “Njoo kwetu bila
kuchelewa”. 39 Petro akaamka na akaondoka pamoja nao. Alipofika, walimleta katika
chumba cha juu. Na wajane wote walisimama karibu naye wakilia, wakimwonyesha
koti na nguo ambazo Dorcas aliwashonea wakati akiwa pamoja nao. 40 Petro
akawatoa wote nje ya chumba, akapiga magoti akaomba, kisha akaugekia mwili,
akasema, “Tabitha, amka”. Akafungua macho yake na alipomwona Petro akakaa
chini. 41 Kisha Petro akampa mkono wake akamwinua, na alipowaita waamini na
wajane, akawakabidhi kwao akiwa hai 42 Jambo hili likajulikana Yafa yote, na watu
wengi wakamwamini Bwana. 43 Ilitokea Petro akakaa siku nyingi Yafa pamoja na
mtu aitwaye Simoni, mtengeneza ngozi.

# 10

1 Kulikuwa na mtu fulani katika mji wa kaisaria, jina lake aliitwa Kornelio, alikuwa
mkuu wa kikosi cha Kiitalia. 2 Alikuwa mchamungu na alimwabudu Mungu na
nyumba yake yote; alitoa pesa nyingi kwa wayahudi na aliomba kwa Mungu siku zote.
3 Muda wa saa tisa za mchana, akaona maono Malaika wa Mungu anakuja kwake.
Malaika akamwambia “Kornelio! 4 Kornelio akamwangalia malaika na alikuwa na
hofu kubwa sana akasema “Hii ni nini mkuu?” Malaika akamwambia “Maombi yako
na zawadi zako kwa masikini zimepanda juu kama kumbukumbu kwenye uwepo
wa Mungu”. 5 Sasa tuma watu kwenda mji wa Yafa kumleta mtu mmoja anayeitwa
Simoni ambaye pia huitwa Petro. 6 Anakaa na mtengenezaji wa Ngozi aitwaye Simoni
ambaye nyumba yake iko kando ya bahari.” 7 Baada ya Malaika aliyekuwa akisema
naye kuondoka, Kornelio akawaita watumishi wa nyumbani kwake wawili, na
askari aliyekuwa akimwabudu Mungu kati ya maaskari waliokuwa wanamtumikia.
8 Kornelio aliwaambia yote yaliyotokea na akawatuma Yafa. 9 Siku iliyofuata muda
wa saa sita wakiwa njiani na wamekaribia mjini, Petro akapanda juu darini kuomba.
10 Na pia akawa na njaa na alihitaji kitu cha kula, lakini wakati watu wanapika
chakula, akaonyeshwa maono, 11 akaona anga limefuguka na chombo kinashuka na
kitu fulani kama nguo kubwa ikishuka chini kwenye ardhi katika kona zake zote nne.
12 Ndani yake kulikuwa na aina zote za wanyama wenye miguu minne na watambaao
juu ya ardhi, na ndege wa angani. 13 Tena sauti ikasema kwake “Amka, Petro chinja
na ule”. 14 Lakini Petro akasema “Siyo hivyo, Bwana kwa sababu sijawahi kula
kitu chochote najisi na kichafu. 15 Lakini sauti ikaja kwake tena kwa mara ya pili
“Alichokitakasa Mungu usikiite najisi wala kichafu”. 16 Hii ilitokea mara tatu, na kile
chombo kikawa kimechukuliwa tena angani. 17 Na wakati Petro akiwa katika hali ya
kuchanganyikiwa juu ya hayo maono yanamaanisha nini, Tazama, watu waliokuwa
wametumwa na Kornelio wakasimama mbele ya lango, wakiuliza njia ya kwenda
kwenye nyumba. 18 Na wakaita na kuuliza kama Simoni ambaye pia aliitwa Petro
kama alikuwa anakaa pale. 19 Wakati huo Petro alipokuwa akiwaza juu ya hayo
maono, Roho akasema naye, “Tazama watu watatu wanakutafuta. 20 Amka na ushuke
chini na uende nao. Usiogope kwenda nao, kwa sababu nimewatuma.” 21 Petro
akashuka chini kwao na kusema “Mimi ni yule mnayemtafuta. Kwa nini mmekuja?”
22 Wakasema, “Akida mmoja jina lake Kornelio, mtu wa haki na hupenda kumwabudu
Mungu, na watu humsema vyema katika taifa lote la kiyahudi, ameambiwa na
malaika wa Mungu kukutuma ili kwenda kwenye nyumba yake, ili asikie ujumbe
kutoka kwako.” 23 Petro akawakaribisha kuingia ndani na kukaa pamoja naye.
Asubuhi iliyofuata akaamka akaenda pamoja naye, na ndugu wachache kutoka Yafa
wakaambatana naye. 24 Siku iliyofuata walikuja Kaisaria. Na Kornelio alikuwa
akiwasubiri; na alikuwa amewaita pamoja ndugu zake na marafiki zake wa karibu.

[25] Wakati Petro akiingia ndani, Kornelio akamlaki na kuinama hadi chini kwenye
miguu yake kwa kumheshimu. [26] Lakini Petro akamwinua na kusema “Simama; mimi
mwenyewe pia ni mwanadamu.” [27] Wakati Petro akiwa anaongea naye, alienda ndani
akakuta watu wamekusanyika pamoja. [28] Akawaambia, “Ninyi wenyewe mnajua
kuwa siyo sheria ya kiyahudi kushirikiana au kutembelewa na mtu ambaye si wa
taifa hili. Lakini Mungu amenionesha mimi kuwa sipaswi kumwita mtu yeyote ni
najisi au mchafu. [29] Na ndiyo maana nimekuja bila kubisha, nilipotumwa kwa ajili ya
hiyo. Kwa hiyo niwaulize kwa nini mlitumwa kwa ajili yangu.” [30] Kornelio akasema,
“Siku nne zilizopita, wakati kama huu nilikuwa naomba muda wa saa tisa mchana
ndani ya nyumba yangu; Nikaona mbele yangu mtu amesimama akiwa na mavazi
meupe, [31] Akaniambia “Kornelio maombi yako yamesikiwa na Mungu, na zawadi
zako kwa masikini zimekuwa ukumbusho mbele za Mungu. [32] Kwa hiyo tuma mtu
Yafa na akamwite mtu mmoja anayeitwa Simoni aje kwako, ambaye pia huitwa Petro.
ambaye anaishi kwa mtengenezaji wa Ngozi mmoja aitwaye Simoni ambaye nyumba
yake iko pembeni mwa bahari. [33] Zingatia: Msatri huu, “Naya atakapokuja atasema
nanyi,” haumo kwenye maandiko ya kale. [34] Ndipo Petro akafungua mdomo wake
na kusema “Kweli, nimeamini kuwa Mungu hawezi kuwa na upendeleo. [35] Badala
yake, kila taifa mtu yeyote anayemwabudu na kufanya matendo ya haki anakubalika
kwake. [36] Unajua ujumbe alioutoa kwa watu wa Israel, alipokuwa akitangaza
habari njema ya amani kupitia Yesu Kristo ambaye ni Bwana wa wote- [37] ninyi
wenyewe mnajua tukio lililotokea, ambalo limetokea Yudea yote na lilianzia Galilaya,
baada ya ubatizo ambao Yohana alitangaza. [38] tukio lililokuwa linamhusu Yesu
Kristo jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na kwa nguvu. Alienda
akifanya mema na kuponya wote walioteswa na ibilsi, kwa kuwa Mungu alikuwa
pamoja naye. [39] Sisi ni mashahidi wa mambo yote aliyoyafanya katika nchi za
Uyahudi na katika Yerusalemu- huyu ni Yesu waliyemuua na kumtundika mtini.
[40] Huyu mtu Mungu alimfufua siku ya tatu na kumpa kujulikana, [41] si kwa watu
wote, lakini kwa mashahidi waliochaguliwa kabla na Mungu. - sisi wenyewe, tulio
kula naye na kunywa naye baada ya kufufuka kutoka kwa wafu. [42] Ametuagiza
kuhubiri kwa watu na kushuhudia kuwa huyu ndiye ambaye Mungu alimchagua
kuwa mwamuzi wa walio hai na waliokufa. [43] Katika yeye manabii wote washuhudie,
ili kwamba kila anayeamini katika yeye atapokea msamaha wa dhambi kupitia jina
lake.” [44] Wakati Petro akiendelea kusema haya, Roho Mtakatifu akawajaza wote
waliokuwa wakisikiliza ujumbe wake. [45] Watu wale wanaohusika na kikundi cha
waamini waliotahiriwa- wale wote waliokuja na Petro- walishangazwa, kwa sababu
ya karama ya Roho Mtakatifu aliyemwagwa pia kwa wamataifa. [46] Kwa kuwa
walisikia hawa wamataifa wanaongea kwa lugha zingine na kumwabudu Mungu.
Petro akajibu, [47] “Kuna mtu yeyote anaweza kuzuia maji ili watu wasibatizwe, Watu
hawa wamempokea Roho Mtakatifu kama sisi?” [48] Ndipo akawaamuru wabatizwe
kwa jina la Yesu Kristo. Baadaye wakamwomba akae nao kwa siku kadhaa.

# 11

[1] Mitume na ndugu wale waliokuwa huko Yudea walisikia kuwa wamataifa
wamelipokea neno la Mungu. [2] Petro alipokuja huko Yerusalemu, lile kundi la
watu waliotahiriwa wakaanza kumkosoa, Wakisema, [3] “Umeshikamana na watu
wasiotahiriwa na kula nao!” [4] Lakini Petro alianza kueleza tukio kwa kina; akisema,
[5] “Nilikuwa naomba katika mji wa Yafa, na nikaona maono ya chombo kikishuka
chini kama nguo kubwa ikishuka kutoka mbinguni katika pembe zake zote nne.
Kikashuka kwangu. [6] Nilikitazama na kufikiri juu yake. Nikaona wanyama wenye
miguu minne waishio katika nchi, na wanyama wa polini na wanyama watambaao

na ndege wa angani. 7 Kisha nikasikia sauti ikisema nami, “Amka, Petro, chinja naj
ule!” 8 Nikasema, “Siyo hivyo, Bwana, mdomoni mwangu hakujawahi kuingia kitu
chochote kisicho kitakatifu au kichafu” 9 Lakini sauti ikajibu tena kutoka Mbinguni,
kile Mungu alichokitangaza kuwa ni safi, usikiite najisi, 10 Hii ilitokea mara tatu, na
kila kitu kikachukuliwa mbinguni tena. 11 Tazama, wakati huo watu watatu walikuwa
wamesimama mbele ya nyumba ile tulimokuwa; wametumwa kutoka Kaisaria kuja
kwangu. 12 Roho akaniambia kwenda nao, na nisitofautiane nao. Hawa wanaume sita
wakaenda pamoja na mimi na tuliende kwenye nyumba ya mtu mmoja. 13 Alituambia
vile alivyomwona malaika amesimama ndani ya nyumba yake akisema, “Nitume
Yafa nikamlete simoni ambaye jina lake lingine ni Petro. 14 Atasema ujumbe kwako
katika huo utaokoka wewe na nyumba yako yote.” 15 Nilipoanza kusema nao, Roho
mtakatifu akaja juu yao kama alivyokuja kwetu mwanzoni. 16 Nakumbuka maneno
ya Bwana, alivyosema, “Yohana alibatiza kwa maji; lakini mtabatizwa katika Roho
mtakatifu.” 17 Pia kama Mungu ametoa zawadi kama alizotupa sisi tulipoamini katika
Bwana Yesu Kristo, mimi ni nani, kwamba naweza kumpinga Mungu? 18 Waliposikia
mambo haya, hawakurudisha, bali walimsifu Mungu na kusema, “Mungu ametoa
toba kwa ajili ya wa mataifa pia” 19 Basi waamini ambao mateso yalianzia kwenye
kifo cha Stephano walitawanyika kutoka Yerusalemu-waamini hawa walienda mbali,
hadi mpaka Foinike, Kipro na Antiokia. Waliwaambia ujumbe kuhusu Yesu peke
yake kwa wayahudi na si kwa mwingine awaye yote. 20 Lakini baadhi yao ni watu
kutoka Kipro na Krene, walikuja Antiokia na kusema na wayunani na kumhubiri
Bwana Yesu. 21 Na mkono wa Bwana ulikuwa pamoja nao, na watu wengi waliamini
na kumgeukia Bwana. 22 Habari zao zikafikia masikioni mwa kanisa la Yerusalem:
na wakamtuma Barnaba aende mpaka Antiokia. 23 Alipokuja na kuona karama ya
Mungu alifurahi; na aliwatia moyo wote kubaki na Bwana katika mioyo yao. 24 Kwa
sababu alikuwa mtu mwema na amejazwa na Roho Mtakatifu na imani na watu
wengi wakaongezeka katika Bwana. 25 Baadaye Barnaba alienda Tarso kumwona
Sauli. 26 Alipompata, akamleta Antiokia. Ikawa kwa mwaka mzima wakakusanyika
pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi wakaitwa wakristo
kwa mara ya kwanza huko Antiokia. 27 Na katika siku hizi manabii wakashuka kutoka
Yerusalemu mpaka Antiokia. 28 Mmoja wao ni Agabo ndilo jina lake, akasimama
akiashiriwa na Roho kuwa njaa kali itatokea ulimwenguni mwote. Hii ilitokea wakati
wa siku za Klaudio. 29 Kwa hiyo, wanafunzi, kila mmoja alivyo fanikiwa, waliamua
kupeleka misaada kwa ndugu walioko Uyahudi. 30 Walifanya hivi; Walituma pesa
kwa mkono wa Barnaba na Sauli.

# 12

1 Wakati huo mfalme Herode akanyosha mkono wake kwa baadhi ya wale
wanaotoka kwenye kusanyiko ili kuwatesa. 2 Akamwuua Yakobo nduguye Yohana
kwa upanga. 3 Baada ya kuona kuwa inawapendeza Wayahudi, akamkamata na
Petro tena. Hii ilikuwa wakati wa mikate isiyochachwa. 4 Alipomkamata, akamweka
gerezani na akaweka vikosi vinne vya askari ili kumlinda, alikuwa akitarajia
kumpeleka kwa watu baada ya Pasaka. 5 Petro akawekwa gerezani, lakini maombi
yakafanywa kwa bidii na kusanyiko kwa ajili yake kwa Mungu. 6 Siku kabla Herode
hajaenda kumtoa, Usiku huo Petro alikuwa amelala katikati ya maaskari wawili,
akiwa amefungwa na minyororo miwili, na walinzi mbele ya mlango walikuwa
wakilinda gereza. 7 Tazama, malaika wa Bwana ghafla akamtokea na nuru ikang'aa
ndani. Akampiga Petro ubavuni na kumwamsha akisema, “Amka haraka.”ndipo
minyororo aliyokuwa amefungwa ikafunguka kutoka mikononi mwake. 8 Malaika
akamwambia, “Vaa nguo zako na vaa viatu vyako.” Petro akafanya hivyo. Malaika

akamwambia, “Vaa vazi lako na unifuate.” 9 Hivyo Petro akamfuata Malaika na
akatoka nje. Hakuamini kilichofanywa na malaika kama ni cha kweli. Alidhani
anaona maono. 10 Baada ya kupita lindo la kwanza na la pili, wakafika kwenye geti
la chuma la kuingilia kwenda mjini, likafunguka lenyewe kwa ajili yao. Wakatoka
nje wakashuka kwenye mtaa, mara Malaika akamwacha. 11 Petro alipojitambua,
akasema, “Sasa nimeamini kuwa Bwana alimtuma Malaika wake ili kunitoa katika
mikono ya Herode, na kwa matarajio ya watu wote wa uyahudi.” 12 Baada ya kujua
haya, akaja kwenye nyumba ya Mariamu mama yake Yohana ambaye ni Marko;
Wakristo wengi walikusanyika wakiomba. 13 Alipobisha kwenye mlango wa kizuizi,
mtumishi mmoja msichana anayeitwa Roda akaja kufungua. 14 Alipotambua ni sauti
ya Petro, kwa furaha akashindwa kuufungua mlango; badala yake, akakimbia ndani
ya chumba; na kuwajulisha kuwa Petro amesimama mbele ya Mlango. 15 Hivyo,
Wakasema kwake, “Wewe ni mwendawazimu” lakini alikazia kuwa ni kweli ni
yeye. Wakasema “Huyo ni malaika wake.” 16 Lakini Petro aliendelea kubisha, na
walipofungua mlango, wakamwona na wakashangaa sana. Petro akawanyamazisha
kwa mkono kimya kimya na akawaambia jinsi Bwana alivyomtoa kutoka Gerezani.
akasema, 17 “Wajulishe haya mambo Yakobo na ndugu zake.” Kisha akaondoka
akaenda sehemu nyingine. 18 Kulipokuwa mchana, kukawa na huzuni kubwa kati
ya askari, kuhusiana na kilichotokea kwa Petro. 19 Baada ya Herode kumtafuta na
hakumwona akawauliza walinzi na akaamuru wauawe. Akaenda kutoka uyahudi
mpaka Kaisaria na kukaa huko. 20 Herode alikuwa na hasira juu ya watu wa Tiro
na Sidoni. Wakaenda kwa pamoja kwake. Wakawa na urafiki na Blasto msaidizi
wa mfalme, ili awasaidie. Kisha wakaomba amani, kwa sababu nchi yao ilipokea
chakula kutoka katika nchi ya mfalme. 21 Siku iliyokusudiwa Herode alivaa mavazi ya
kifalme na kukaa kwenye kiti chake cha kifalme, na akawahutubia. 22 Watu wakapiga
kelele, “Hii ni sauti ya mungu wala si sauti ya mwanadamu!” 23 Mara ghafla malaika
akampiga, kwa sababu alikuwa hakumpa Mungu utukufu; akaliwa na chango na
akafa 24 Lakini neno la Mungu likakua na kusambaa. 25 Baada ya Barnaba na Sauli
kukamilisha huduma yao wakatoka pale wakarejea Yerusalemu, wakamchukua na
Yohana ambaye jina la kuzaliwa ni Marko.

# 13

1 Sasa katika kanisa la Antiokia, palikuwa na baadhi ya manabii na walimu.
Walikua Barnaba, Simeoni (aliyeitwa Nigeri). Lukio wa Kirene, Manaeni( ndugu
asiye wa damu wa Herode kiongozi wa mkoa), na Sauli. 2 Walipokuwa wakimwabudu
Bwana na kufunga, Roho Mtakatifu alisema, “Niteengeeni pembeni Barnaba na Sauli,
waifanye kazi niliyo waitia.” 3 Baada ya Kanisa kufunga, kuomba, na kuweka mikono
yao juu ya watu hawa, wakawaacha waende. 4 Kwa hiyo Barnabas na Sauli walimtii
Roho Mtakatifu na walitelemka kuelekea Seleukia; Kutoka huko walisafiri baharini
kuelekea kisiwa cha Kipro. 5 Walipokuwa katika mji wa Salami, walilitangaza neno
la Mungu katika Masinagogi ya Wayahudi. Pia walikuwa pamoja na Yohana Marko
kama msaidizi wao. 6 Walipokwenda katika kisiwa chote mpaka Pafo, walikuta
mtu fulani mchawi, Myahudi nabii wa uongo, ambaye jina lake lilikuwa Bar Yesu.
7 Mchawi huyu alishirikiana na Liwali Sergio Paulus, aliyekuwa mtu mwenye akili.
Mtu huyu aliwaalika Barnaba na Sauli, kwa sababu alihitaji kusikia neno la Mungu.
8 Lakini Elima “yule mchawi” (hivyo ndivyo jina lake lilivyo tafsiriwa) aliwapinga;
alijaribu kumgeuza yule liwali atoke kwenye imani. 9 Lakini Sauli aliyeitwa Paulo,
alikuwa amejazwa na Roho Mtakatikfu, akamkazia macho 10 na akasema “Ewe
mwana wa Ibilisi, umejazwa na aina zote za udanganyifu na udhaifu. Wewe ni adui
wa kila aina ya haki. Hautakoma kuzigeuza njia za Bwana, zilizonyooka, je utaweza?

[11] Sasa tazama, mkono wa Bwana upo juu yako, na utakuwa kipofu. Hautaliona Jua
kwa muda" mara moja ukungu na giza vilianguka juu ya Elimas; alianza kuzunguka
pale akiomba watu wamwongoze kwa kumshika mkono. [12] Baada ya liwali kuona
kilichotokea, aliamini, kwa sababu alishangazwa kwa mafundisho kuhusu Bwana.
[13] Sasa Paulo na rafiki zake walisafiri majini kutoka Pafo na wakafika Perge katika
Pamfilia. Lakini Yohana aliwaacha na kurudi Yerusalemu. [14] Paulo na rafiki yake
walisafiri kutoka Perge na wakafika Antiokia ya Pisidia. Huko walikwenda katika
sinagogi siku ya Sabato na kukaa chini. [15] Baada ya kusoma sheria na manabii,
viongozi wa sinagogi aliwatumia ujumbe wakisema, "Ndugu, kama mnao ujumbe wa
kutia moyo watu hapa, semeni" [16] Kwa hiyo Paulo alisimama na kuwapungia mkono;
alisema, "Wanaume wa Israeli na enyi mnao mtii Mungu, sikilizeni. [17] Mungu wa
hawa watu wa Israeli aliwachagua baba zetu na kuwafanya watu wengi walipokaa
katika nchi Misri, na kwa mkono wake kuinuliwa aliwaongoza nje yake. [18] Kwa
miaka arobaini aliwavumilia katika jangwa. [19] Baada ya kuyaharibu mataifa saba
katika nchi ya Kaanani, aliwapa watu wetu nchi yao kwa urithi. [20] Matukio haya
yote yalitokea zaidi ya miaka mia nne na hamsini. Baada ya vitu hivi vyote, Mungu
aliwapa waamuzi mpaka Samweli Nabii. [21] Baada ya haya, watu waliomba mfalme,
hivyo Mungu aliwapa Sauli mwana wa Kishi, mtu wa kabila la Benjamini, kuwa
mfalme kwa miaka arobaini. [22] Kisha baada ya Mungu kumuondoa katika ufalme,
alimwinua Daudi kuwa mfalme wao. Ilikuwa ni kuhusu Daudi kwamba Mungu
alisema, 'Nimempata Daudi mwana wa Yese kuwa mtu apendezwaye na moyo wangu;
ambaye atafanya kila kitu nipendacho.' [23] Kutoka kwenye ukoo wa mtu huyu Mungu
ameiletea Israeli mkombozi, Yesu, kama alivyoahidi kufanya. [24] Hili lilianza kutokea,
kabla ya Yesu kuja, Yohana kwanza alitangaza ubatizo wa toba kwa watu wote wa
Israeli. [25] Naye Yohana alipokuwa akimalizia kazi yake, alisema, 'Mwanifikiri mimi
ni nani? mimi si yule. Lakini sikilizeni, ajaye nyuma yangu, sisitahili kulegeza viatu
vya miguu yake.' [26] Ndugu, watoto wa ukoo wa Abrahamu, na wale ambao kati
yenu mnamwabudu Mungu, ni kwa ajili yetu kwamba ujumbe huu wa ukombozi
umetumwa. [27] Kwa wale waishio Yerusalemu, na watawala wao, hawakumtambua
kwa uhalisia, na wala hawakuutambua ujumbe wa manabii ambao husomwa kila
Sabato; kwa hiyo walitimiliza ujumbe wa manabii kwa kumhukumu kifo Yesu.
[28] Japokuwa hawakupata sababu nzuri kwa kifo ndani yake, walimwomba Pilato
amuue. [29] Walipomaliza mambo yote yaliyoandikwa kuhusu yeye, walimshusha
kutoka mtini na kumlaza kaburini. [30] Lakini Mungu alimfufua kutoka wafu.
[31] Alionekana kwa siku nyingi kwa wale waliokwenda pamoja naye kutoka Galilaya
kuelekea Yerusalemu. Watu hawa sasa ni mashahidi wa watu. [32] Hivyo tunawaletea
habari njema kuhusu ahadi walizopewa mababu zetu. [33] Mungu aliweka ahadi hizi
kwetu, watoto wao, katika hilo alimfufua Yesu na kumrudisha tena katika uhai. Hili
pia liliandikwa katika Zaburi ya pili: 'Wewe ni Mwanangu, leo nimekuwa Baba
yako' [34] Pia kuhusu ukweli ni kwamba alimfufua kutoka wafu ili kwamba mwili
wake usiharibike, ameongea hivi: 'Nitakupatia utakatifu na baraka halisi za Daudi'
[35] Hii ndiyo sababu kasema pia katika zaburi nyingine, 'Hautaruhusu mtakatifu
wako kuuona uozo.' [36] Kwa kuwa baada ya Daudi kutumikia mapenzi ya Mungu
katika kizazi chake, alilala, alilazwa pamoja na baba zake, na aliuona uaharibifu,
[37] Lakini aliyefufuliwa na Mungu hakuuona uharibifu. [38] Hivyo na ifahamike kwenu,
ndugu, kupitia mtu huyu, msamaha wa dhambi umehubiriwa. [39] Kwa yeye kila
aaminiye anahesabiwa haki na mambo yote ambayo sheria ya Musa isingewapatia
haki. [40] Hivyo basi kuweni waangalifu kwamba kitu walichokiongelea manabii
kisitokee kwenu: [41] 'Tazama, enyi mnaodharau, na mkashangae na mkaangamie;
kwa vile nafanya kazi katika siku zenu, Kazi ambayo hamwezi kuiamini, hata kama

mtu atawaeleza.” 42 Wakati Paulo na Barnaba walipoondoka, watu wakawaomba
waongee maneno haya siku ya Sabato ijayo. 43 Wakati mkutano wa sinagogi
ulipokwisha, Wayahudi wengi na waongofu thabiti waliwafuata Paulo na Barnaba,
ambao waliongea nao na waliwahimiza waendelee katika neema ya Mungu. 44 Sabato
iliyofuata, karibu mji mzima ulikusanyika kusikia neno la Mungu. 45 Wayahudi
walipoona makutano, walijawa na wivu na kuongea maneno yaliyopinga vitu
vilivyosemwa na Paulo na walimtukana. 46 Lakini Paulo na Barnaba waliongea
kwa ujasiri na kusema, “Ilikuwa ni muhimu kwamba neno la Mungu liongelewe
kwanza kwenu. Kwa kuwa mnalisukumia mbali kutoka kwenu nakujiona kuwa
hamkusitahili uzima wa milele, angalieni tutawageukia Mataifa. 47 Kama ambavyo
Bwana ametuamuru, akisema, 'Nimewaweka ninyi kama nuru kwa watu wa mataifa,
kwamba mlete wokovu kwa pande zote za dunia.” 48 Mataifa waliposikia hili,
walifurahi na kulisifu neno la Bwana. Wengi waliochaguliwa kwa uzima wa milele
waliamini. 49 Neno la Bwana lilienea nchi yote. 50 Lakini wayahudi waliwasihi
waliojitoa na wanawake muhimu, pia na viongozi wa mji. Haya yalichochea mateso
dhidi ya Paulo na Barnaba na waliwatupa nje ya mipaka ya mji. 51 Lakini Paulo na
Barnaba walikung'uta vumbi ya miguu yao. Kisha walienda kwenye mji wa Ikonia.
52 Na wanafunzi walijawa na furaha pamoja na Roho mtakatifu.

# 14

1 Ikatokea ndani ya Ikonio kwamba Paulo na Barnaba waliingia pamoja ndani ya
sinagogi la Wayahudi nakuongea namna ambayo kundi kubwa la watu Wayahudi
na Wayunani waliamini. 2 Lakini wayahudi wasiotii waliwachochea akili wamataifa
na kuwafanya kuwa wabaya dhidi ya ndugu. 3 Kwa hiyo walikaa huko kwa muda
mrefu, wakiongea kwa ujasiri kwa nguvu ya Bwana, huku akitoa uthibitisho kuhusu
ujumbe wa neema yake. Alifanya hivi kwa kutoa ishara na majaabu vifanywe kwa
mikono ya Paulo na Barnaba. 4 Lakini eneo kubwa la mji liligawanyika: baadhi
ya watu walikuwa pamoja na Wayahudi, na baadhi pamoja na mitume. 5 Wakati
wamataifa na Wayahudi walipojaribu kuwashawishi viongozi wao kuwatendea
vibaya na kuwaponda mawe Paulo na Barnaba, 6 wakalitambua hilo na kukimbilia
katika miji ya Likaonia, Listra na Derbe, na maeneo yanayozunguka pale, 7 na
huko waliihubiri injili. 8 Na huko Listra palikuwa na mtu mmoja aliyekaa, hakuwa
na nguvu miguuni mwake, kilema kutoka tumboni mwa mama yake, hajawahi
kutembea. 9 Mtu huyu alimsikia Paulo akiongea. Paulo alimkazia macho na akaona
kwamba alikuwa na imani ya kuponywa. 10 Hivyo alisema kwake kwa sauti ya
juu, “Simama kwa miguu yako.” Na yule mtu aliruka juu na kuanza kutembea.
11 Umati ulipoona alichokifanya Paulo, waliinua sauti zao, wakisema katika lahaja
ya Kilikaonio, “miungu imetushukia kwa namna ya binadamu.” 12 Walimwita
Barnaba “Zeu,” na Paulo “Herme” kwa sababu alikuwa msemaji mkuu. 13 Kuhani
wa Zeu, ambaye hekalu lake lilikuwa nje ya mji, alileta fahari la ng'ombe na
mtungo wa maua mpaka kwenye lango la mji, yeye na umati walitaka kutoa sadaka.
14 Lakini mitume, Barnaba na Paulo, walipolisikia hili, walirarua mavazi yao na kwa
haraka walikwenda nje kwenye umati, wakilia 15 na kusema, “Enyi watu, kwanini
mnafanya mambo haya? Na sisi pia ni binadamu wenye hisia kama za kwenu.
Tunawaletea habari njema, kwamba mgeuke kutoka kwenye vitu hivi visivyofaa
na kumwelekea Mungu aliye hai, aliyeumba mbingu, dunia na bahari na kila kitu
kilichomo. 16 Katika nyakati zilizopita, aliwaruhusu mataifa kutembea katika njia
zao wenyewe. 17 Lakini bado, hakuondoka pasipo shahidi, katika hilo alifanya vizuri
na akawapatia mvua kutoka mbinguni na nyakati za mazao, akiwajaza mioyo yenu
kwa vyakula na furaha” 18 Hata kwa maneno haya, Paulo na Barnaba kwa shida

waliuzuia umati kuwatolea sadaka. [19] Lakini baadhi ya Wayahudi kutoka Antiokia
na Ikonio walikuja kuushawishi umati. Wakampiga mawe Paulo na kumburuta
hadi nje ya mji, wakidhani alikuwa amekufa. [20] Hata hivyo wanafunzi walikuwa
wamesimama karibu naye, aliamka, wakaingia mjini. Siku ya pili, aliende Derbe
na Barnaba. [21] Baada ya kufundisha injili katika mji ule na kuwafanya wanafunzi
wengi, walirudi Listra, hadi Ikoniamu, na hadi Antiokia. [22] Waliendelea kuimarisha
nafsi za wanafunzi na kutiwa moyo kuendelea katika imani, akasema, "Lazima
tuingie katika ufalme wa Mungu kwa kupitia mateso mengi." [23] Walipo wateua
kwa ajili yao wazee wa kila kusanyiko la waaminio, na wakiwa wameomba na
kufunga, waliwakabidhi kwa Bwana, ambaye wao walimwamini. [24] Kisha walipita
katika Pisidia, walifika Pamfilia. [25] Wakati walipoongea maneno katika Perga,
waliteremka kwenda Atalia. [26] Kutoka huko walipanda meli hadi Antiokia ambako
walikuwa wamejitoa kwa neema ya Mungu kwa ajili ya kazi ambayo sasa walikuwa
wameikamilisha. [27] Walipofika huko Antiokia, na kulikusanya kusanyiko la pamoja,
wakatoa taarifa ya mambo ambayo Mungu amefanya kwao, na jinsi alivyowafungulia
mlango wa imani kwa watu wa Mataifa. [28] Walikaa kwa muda mrefu na wanafunzi.

# 15

[1] Watu fulani walishuka kutoka Uyahudi na kuwafundisha ndugu, wakisema,
"msipotahiriwa kama desturi ya Musa, hamwezi kuokolewa." [2] Wakati Paulo na
Barnaba walipokuwa na mapambano na mjadala pamoja nao, ndugu waliamua
kwamba Paulo, Barnaba, na wengine kadhaa waende Yerusalem kwa mitume
na wazee kwa ajili ya swali hili. [3] Kwa hiyo, kwa kutumwa kwao na kanisa,
walipitia Foinike na Samaria wakitangaza kugeuzwa nia kwa wamataifa. Walileta
furaha kuu kwa ndugu wote, [4] Walipokuja Yerusalem, walikaribishwa na Kanisa
na mitume na wazee, na waliwasilisha taarifa ya mambo yote ambayo Mungu
amefanya pamoja nao. [5] Lakini watu fulani walioamini, waliokuwa katika kundi
la Mafarisayo, walisimama nakusema, "ni muhimu kuwatahiri na kuwaamuru
waishike sheria ya Musa." [6] Hivyo mitume na wazee walisimama pamoja kulifikiria
hili swala. [7] Baada ya majadiliano marefu, Petro alisimama na kusema kwao,
"Ndugu mwatambua kwamba kitambo kizuri kilichopita Mungu alifanya chaguo
kati yenu, kwamba kwa mdomo wangu Mataifa wasikie neno la injili, na kuamini.
[8] Mungu, anayefahamu mioyo, anashuhudia kwao, anawapa Roho mtakatifu, kama
alivyofanya kwetu; [9] na hakutengeneza utofauti kati yetu na wao, akiifanya mioyo
yao safi kwa imani. [10] Kwa hiyo, kwa nini mnamjaribu Mungu kwamba muweke
nira juu ya shingo za wanafunzi ambayo hata baba zetu wala sisi hatukuweza
kustahimili? [11] Lakini twaamini kwamba tutaokolewa kwa neema ya Bwana Yesu,
kama walivyokuwa." [12] Kusanyiko lote lilinyamaza walipokua wakimsikiliza Barnaba
na Paulo walipokuwa wakitoa taarifa ya ishara na maajabu ambayo Mungu alifanya
pamoja nao kati ya watu wa mataifa. [13] Walipoacha kuongea, Yakobo alijibu
akisema, "Ndugu nisikilizeni. [14] Simoni ameelezea jinsi kwanza Mungu kwa neema
aliwasaidia Mataifa ili kwamba ajipatie kutoka kwao watu kwa ajili ya jina lake.
[15] Maneno ya manabii yanakubaliana na hili kama lilivyoandikwa. [16] 'Baada ya
mambo haya nitarudi na kuijenga tena hema ya Daudi, iliyoanguka chini; nitainua
na kuhuisha uhararibifu wake, [17] ili kwamba watu waliobaki wamtafute Bwana,
pamoja na watu wa Mataifa walioitwa kwa jina langu.' [18] Hivi ndivyo asemavyo
Bwana aliyefanya mambo haya yajulikanayo tangu enzi za zamani. [19] Hivyo
basi, ushauri wangu ni, kwamba tusiwapatie shida watu wa Mataifa wamgeukiao
Mungu; [20] lakini tuandike kwao kwamba wajiepushe mbali na uharibifu wa sanamu,
tamaa za uasherati, na vilivyonyongwa, na damu. [21] Kutoka vizazi vya wazee

kuna watu katika kila mji wahubirio na kumsoma Musa katika masinagogi kila
Sabato.” 22 Kwa hiyo ikaonekana kuwa imewapendeza mitume na wazee, pamoja
na kanisa lote, kumchagua Yuda aliyeitwa Barsaba, na Silas, waliokuwa viongozi
wa kanisa, na kuwatuma Antiokia pamoja na Paulo na Barnaba. 23 Waliandika
hivi, “Mitume, wazee na ndugu, kwa ndugu wa Mataifa walioko Antiokia, Shamu
na Kilikia, salamu. 24 Tulisika kwamba watu fulani ambao hatukuwapatia amri
hiyo, walitoka kwetu na wamewataabisha kwa mafundisho yaletayo shida nafsini
mwenu. 25 Kwa hiyo imeonekana vyema kwetu sote kuchagua watu na kuwatuma
kwenu pamoja na wapendwa wetu Barnaba na Paulo, 26 watu walio hatarisha
maisha yao kwa ajili ya jina la Bwana Yesu Kristo. 27 Kwa hiyo tumemtuma
Yuda na Sila, watawaambia mambo yayo hayo. 28 Kwa kuwa ilionekana vyema
kwa Roho Mtakatifu na kwetu, kutoweka juu yenu mzigo mkubwa kuliko mambo
haya yaliyo ya lazima: 29 kwamba mgeuke kutoka kwenye vitu vitolewavyo kwa
sanamu, damu, vitu vya kunyongwa, na uasherati. Kama mtajiweka mbali na
hivi, itakuwa vyema kwenu. Kwa herini.” 30 Hivyo basi, walivyotawanyishwa,
waliteremkia Antiokia; baada ya kukusanya kusanyiko pamoja, waliwasilisha barua.
31 Walipokua wameisoma, walifurahi kwa sababu ya kutiwa moyo. 32 Yuda na Sila,
na manabii, waliwatia moyo ndugu kwa maneno mengi na kuwatia nguvu. 33 Baada
ya kukaa muda fulani huko, walitawanyishwa kwa amani kutoka kwa ndugu kwa
wale waliowatuma. 34 [ Lakini ilionekana vyema Sila kubaki huko ] 35 Lakini Paulo
na wengine walikaa Antiokia pamoja na wengine wengi, ambapo walifundisha na
kuhubiri neno la Bwana. 36 Baada ya siku kadhaa Paulo alisema kwa Barnaba, “Na
turudi sasa na kuwatembelea ndugu katika kila mji tulipohubiri neno la Bwana, na
kuwaona walivyo. 37 Barnaba alihitaji pia kumchukua pamoja nao Yohana aliyeitwa
Marko. 38 Lakini Paulo alifikiria haikuwa vizuri kumchukua Marko, aliyewaacha
huko Pamfilia na hakuendelea nao katika kazi. 39 Kisha hapo kukatokea mabishano
makubwa kwa hiyo walitengana, na Barnaba alimchukua Marko na kusafiri kwa meli
mpaka Kipro, 40 Lakini Paulo alimchagua Sila na kuondoka, baada ya kukabidhiwa na
ndugu katika neema ya Bwana. 41 Na alienda kupitia Shamu na Kilikia, akiimarisha
makanisa.

# 16

1 Paulo pia alipokuja Derbe na Lystra; na tazama, pale palikuwepo na mwanafunzi
aitwaye Timotheo, ni Kijana aliyezaliwa na mama wa Kiyahudi ambaye ni muumini
na baba yake ni Mgiriki. 2 Watu wa Listra na Ikonia walimshudia vizuri.
3 Paulo alimtaka ili asafiri naye, hivyo akamchukua na kumtahiri kwa sababu ya
Wayahudi waliokuwako huko kwani wote walimjua kuwa baba yake ni Mgiriki.
4 Walipokuwa wakienda walipita kwenye miji na kutoa maagizo kwa makanisa ili
kuyatii maagizo hayo yaliandikwa na mitume na wazee huko Yerusalemu. 5 Hivyo
makanisa yakaimarishwa katika imani na walioamini wakaongezeka kwa idadi kila
siku. 6 Paulo na mwenzake wakaenda Firigia na Galatia, kwani Roho wa Mungu
aliwakataza kuhubiri neno huko kwenye jimbo la Asia. 7 Walipokaribia Misia,
walijaribu kwenda Bithinia, lakini Roho wa Yesu akawakataza. 8 Kwa hiyo wakapita
Misia wakaja mpaka Mji wa Troa. 9 Maono yalimtokea Paulo usiku, kulikuwa na mtu
wa Makedonia amesimama, akimwita na kusema “Njoni mtusaidie huku Makedonia”.
10 Paulo alipoona maono, mara tukajiandaa kwenda Makedonia, akijua kwamba
Mungu alituita kwenda kuwahubiria injili. 11 Hivyo tukaondoka kutoka Troa,
tukaenda moja kwa moja Samothrake, na siku iliyofuata tukafika mji wa Neapoli.
12 Kutoka hapo tukaenda Filipi ambao ni moja ya mji wa Makedonia, mji muhimu
katika wilaya na utawala wa Kirumi na tukakaa siku kadhaa. 13 Siku ya Sabato,

tulikwenda nje ya lango kwa njia ya mto, sehemu ambayo tulidhania kutakuwa na
mahali pa kufanyia maombi. Tulikaa chini na kuongea na akinamama waliokuja
pamoja. [14] Mwanamke mmoja aitwaye Lidia, muuzaji wa zambarau, kutoka katika
mji wa Tiatira, mwenye kumwabudu Mungu, alitusikiliza. Bwana alimfungua moyo
wake na kuweka maanani maneno yaliyosemwa na Paulo. [15] Baada ya kubatizwa,
yeye na nyumba yake yote, alitusihi akisema " kama mmeniona kuwa mimi ni
mwaminifu katika Bwana, basi nawasihi muingie na kukaa kwangu". Akatusihi
sana. [16] Ikawa kwamba, tulipokuwa tunaenda mahali pa kuomba, msichana mmoja
aliyekuwa na pepo la utambuzi akakutana nasi. Alimletea bwana wake faida nyingi
kwa kubashiri. [17] Mwanamke huyu alimfuata Paulo pamoja na sisi, akipiga kelele na
kusema "Hawa wanaume ni watumishi wa Mungu aliye Mkuu, wanaowatangazia
ninyi habari ya wokovu". [18] Alifanya hivyo kwa siku nyingi, lakini Paulo akiwa
amekasirishwa na tendo hilo, aligeuka nyuma na kumwambia pepo, " Nakuamuru
kwa Jina la Yesu umtoke ndani yake." Naye akatoka na kumwacha mara moja.
[19] Mabwana zake walipoona ya kuwa tumaini la faida yao limeondoka, waliwakamata
Paulo na Sila na kuwaburuza sokoni mbele ya wenye mamlaka. [20] Walipowafikisha
kwa mahakimu, walisema, "Hawa wanaume ni Wayahudi na wanasababisha ghasia
kubwa katika mji wetu. [21] Wanafundisha mambo ambayo siyo sheria sisi kuyapokea
wala kuyafuata kama Warumi." [22] Umati ukawainukia kinyume Paulo na Sila,
mahakimu wakararua nguo zao na kuwavua na kuamuru wachapwe viboko [23] Baada
ya kuwachapa viboko vingi, waliwatupa gerezani na kumuamuru askari wa gereza
kuwalinda vyema. [24] Baada ya kupokea amri hiyo, askari wa gereza aliwatupa
katika chumba cha ndani ya gereza na kuwafunga miguu yao kwenye sehemu
alipowahifadhi. [25] Wakati wa usiku wa manane, Paulo na Sila wakawa wakiomba
na kuimba nyimbo za kumsifu Mungu, huku wafungwa wengine wakiwasikiliza,
[26] Ghafla kukatokea tetemeko kuu na misingi ya gereza ikatikiswa, milango ya gereza
ikafunguka, na minyororo ya wafungwa wote ikalegezwa. [27] Mlinzi wa Gereza
aliamka kutoka usingizini na akaona milango yote ya gereza imefunguliwa; hivyo
akachukua upanga wake maana alitaka kujiua kwa sababu alifikiri wafungwa wote
walikwishatoroka, [28] Lakini, Paulo akapiga kelele kwa sauti kuu, akisema "usijidhuru
kwa sababu wote tuko mahali hapa". [29] Mlinzi wa gereza aliomba taa ziletwe
na akaingia ndani ya gereza kwa haraka, akitetemeka na kuogopa, akawaangukia
Paulo na Sila, [30] na kuwatoa nje ya gereza na kusema, "Waheshimiwa, nifanye
nini ili nipate kuokoka?" [31] Nao wakamwambia, "Mwamini Bwana Yesu nawe
utaokoka pamoja na nyumba yako." [32] Walinena neno la Bwana kwake, pamoja
na watu wote wa nyumbani kwake, [33] Mlinzi wa gereza aliwachukua usiku ule
na kuwaosha sehemu walizoumia, yeye pamoja na watu wa nyumbani mwake
wakabatizwa mara. [34] Akawaleta Paulo na Sila nyumbani kwake na kuwatengea
chakula. Naye akawa na furaha kuu pamoja na watu wa nyumbani mwake kwa
sababu walimwamini Mungu. [35] Ilipokuwa mchana, mahakimu walituma ujumbe
kwa yule mlinzi wa gereza wakisema, "Waruhusu wale watu waende", [36] Mlinzi
wa gereza akamjulisha Paulo juu ya maneno hayo ya kuwa, "Mahakimu walituma
ujumbe niruhusu mwondoke: hivyo tokeni nje na mwende kwa amani." [37] Lakini
Paulo akawaambia, "Walitupiga hadharani, watu ambao ni Warumi bila kutuhukumu
na waliamua kututupa gerezani; halafu sasa wanataka kututoa kwa siri? Hapana,
haitawezekana, wao wenyewe waje kututoa mahali hapa". [38] Walinzi wakawajulisha
mahakimu juu ya maneno hayo, mahakimu wakaogopa sana pale walipojua kuwa
Paulo na Sila ni Warumi. [39] Mahakimu wakaja na kuwasihi watoke, na walipowatoa
nje ya gereza, waliwaomba Paulo na Sila watoke nje ya mji wao. [40] Kwa hiyo Paulo na
Sila wakatoka nje ya gereza wakaja nyumbani kwa Lidia. Paulo na Sila walipowaona

ndugu, waliwatia moyo na kisha kuondoka katika mji huo.

# 17

[1] Na walipopita katika miji ya Amfipoli na Apolonia, walikuja mpaka mji wa The-
salonike ambao kulikuwa na sinagogi la Wayahudi. [2] Kama ilivyo kawaida ya Paulo,
alienda kwao, na kwa muda wa siku tatu za Sabato alijadiliana nao juu ya maandiko.
[3] Alikuwa akiwafungulia maandiko na kuwaeleza kuwa, ilimpasa Kristo ateseke na
kisha kufufuka tena kutoka kwa wafu. Aliwaambia, "Huyu Yesu ninayewaambia
habari zake ndiye Kristo" [4] Baadhi ya Wayahudi walishawishika na kuungana na
Paulo na Sila, pamoja na Wagiriki wachamungu, akinamama wengi waongofu na
kundi kubwa la watu. [5] Lakini baadhi ya Wayahudi wasioamini, waliojawa na
wivu, walienda sokoni na kuwachukuwa baadhi ya watu waovu, wakakusanya
umati wa watu pamoja, na kusababisha ghasia mjini, kisha wakaivamia nyumba
ya Jason, wakitaka kuwakamata Paulo na Sila ilikuwaleta mbele za watu. [6] Lakini
walipowakosa, walimkamata Yasoni na baadhi ya ndugu wengine na kuwapeleka
mbele ya maofisa wa mji, wakipiga kelele, " Hawa wanaume walioupindua
ulimwengu wamefika mpaka huku pia, [7] Wanaume hawa waliokaribishwa na Yasoni
wanaihalifu sheria ya Kaisari, wanasema kuna mfalme mwingine anayeitwa Yesu"
[8] Umati na maofisa wa mji waliposikia mambo hayo, waliingiwa na wasiwasi. [9] Baada
ya kuwa wamekwisha kuchukua fedha ya thamani ya ulinzi kutoka kwa Yason na
wengine, waliwaachia waende. [10] Usiku ule ndugu walimtuma Paulo na Sila Beroya.
Na walipofika kule walikwenda katika sinagogi la Wayahudi. [11] Watu wale walikuwa
wenye werevu mkubwa kuliko wale watu wa Thesalonike, kwa sababu walikuwa
na utayari wa kulipokea neno kwa akili zao, na kuchunguza maandiko kila siku ili
kuona kama maneno yaliyonenwa ndivyo yalivyo. [12] Kwa hiyo wengi wao waliamini,
wakiwemo wanawake wenye ushawishi mkubwa wa Kigiriki na wanaume wengi.
[13] Lakini Wayahudi wa Thesalonike walipogundua kwamba Paulo anatangaza neno
la Mungu huko Beroya, walienda huko na kuchochea na kisha kuanzisha ghasia
kwa watu. [14] Kwa haraka, ndugu wakampeleka Paulo kwa njia ya ziwa, lakini
Sila na Timotheo wakabaki pale. [15] Wale ndugu waliompeleka Paulo walienda naye
hadi Athene, walipomwacha Paulo huko, walipokea maagizo kutoka kwake kuwa,
Sila na Timotheo waje kwake kwa haraka iwezeanavyo. [16] Na wakati akiwasubiri
huko Athene, roho yake ilikasirishwa ndani yake kwa jinsi alivyouona mji ulivyojaa
sanamu nyingi. [17] Hivyo akajadiliana katika sinagogi na wayahudi wale waliomcha
Mungu na kwa wale wote aliokutana nao kila siku sokoni. [18] Lakini baathi ya
Wanafalsafa wa Waepikureo na Wastoiko wakamkabili. Na wengine wakasema, "
Ni nini anachokisema huyu mwongeaji mchanga? Wengine wakasema, "inaonekana
anahubiri habari ya mungu mgeni," kwasababu anahubiri habari ya Yesu na ufufuo.
[19] Wakamchukua Paulo na kumleta Areopago, wakisema, "Twaweza kujua haya
mafundisho mapya unayoyaongea? [20] Kwasababu unaleta mambo mapya katika
masikio yetu. Kwahivyo tunataka kujua haya mambo yana maana gani?" [21] (Na watu
wote wa Athene pamoja na wageni waliopo kwao, hutumia muda wao aidha katika
kuongea na kusikiliza juu ya jambo jipya.) [22] Kwa hiyo Paulo akasimama katikati ya
watu wa Areopago na kusema, "Enyi watu wa Athene, naona kuwa ninyi ni watu
wa dini kwa kila namna, [23] Kwani katika kupita kwangu na kuangalia vitu vyenu vya
kuabudu, nimeona maneno yalioandikwa kwenye moja ya madhabahu yenu, ikisema
"KWA MUNGU ASIYEJULIKANA". Hivyo basi, huyo mnayemwabudu pasipokujua,
ndiye ninayewajulisha ninyi. [24] Mungu aliyeumba dunia na kila kitu kilichoko
ndani, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hawezi kukaa katika mahekalu
yaliyotengenezwa na mikono. [25] Na pia hatumikiwi na mikono ya wanadamu kana

kwamba anahitaji kitu kwao, kwani yeye mwenyewe huwapa watu uzima na pumzi
na vitu vingine vyote. 26 Kupitia mtu mmoja, alifanya mataifa yote ya watu waishio
juu ya uso wa dunia, na akawawekea nyakati na mipaka katika maeneo wanaoishi.
27 Kwa hiyo, wanatakiwa kumtafuta Mungu, na yamkini wamfikie na kumpata, na
kwa uhakika hayupo mbali na kila mmoja wetu. 28 Kwake tunaishi, tunatembea
na kuwa na uzima wetu, kama vile mtunzi wenu mmoja wa shairi aliposema 'tu
wazaliwa wake.' 29 Kwa hiyo, ikiwa sisi ni wazaliwa wa Mungu, hatupaswi kufikiri
kuwa uungu ni kama dhahabu, au shaba, au mawe, sanamu iliyochongwa kwa ustadi
na mawazo ya watu. 30 Kwa hiyo, Mungu alinyamazia nyakati zile za ujinga, lakini
sasa anaamuru watu wote kila mahali wapate kutubu. 31 Hii ni kwa sababu ameweka
siku atakayo ihukumu dunia kwa haki kwa mtu ambaye alimchagua. Mungu alitoa
uhakika wa mtu huyu kwa kila mtu pale alipomfufua katoka kwa wafu. 32 Na watu
wa Athene waliposikia habari ya kufufuliwa kwa wafu, baadhi yao wakamdhihaki
Paulo, ila wengine wakasema “Tutakusikiliza tena kwa habari ya jambo hili” 33 Baada
ya hapo, Paulo akawaacha. 34 Lakini baadhi ya watu waliungana naye wakaamini,
akiwemo Dionisio Mwareopago, na Mwanamke anaitwa Damari na wengine pamoja
nao.

# 18

1 Baada ya mambo hayo, Paulo aliondoka Athene kwenda Korintho. 2 Huko
akampata Myahudi aitwaye Akwila mtu wa kabila la Ponto, yeye na mke wake
aitwaye Prisila walikuja kutoka huko Italia, kwa sababu Klaudia aliamuru Wayahudi
wote waondoke Roma; Paulo akaja kwao; 3 Paulo akaishi na kufanya kazi nao kwani
yeye anafanya kazi inayofanana na yao. Wao walikuwa ni watengeneza mahema.
4 Paulo akajadiliana nao katika sinagogi kila siku ya Sabato. Aliwashawishi Wayahudi
pamoja na Wagiriki. 5 Lakini Sila na Timotheo walipokuja kutoka Makedonia, Paulo
alisukumwa na Roho kuwashuhudia Wayahudi kuwa Yesu ndiye Kristo. 6 Wakati
Wayahudi walipompinga na kumdhihaki, hivyo Paulo akakung'uta vazi lake mbele
yao, na kuwaambia, “Damu yenu na iwe juu ya vichwa vyenu wenyewe; Mimi
sina hatia. Kutoka sasa na kuendelea, nawaendea Mataifa”. 7 Hivyo akaondoka
kutoka pale akaenda kwenye nyumba ya Tito Yusto, Mtu anayemwabudu Mungu.
Nyumba yake iko karibu na sinagogi. 8 Krispo, kiongozi wa sinagogi pamoja
na watu wa nyumbani mwake wakamwamini Bwana. Watu wengi wa Korintho
waliomsikia Paulo akiongea waliamini na kubatizwa. 9 Bwana akamwambia Paulo
usiku kwa njia ya maono, “Usiogope, lakini ongea na usinyamaze. 10 Kwani Mimi
niko pamoja nawe, na hakuna atakayejaribu kukudhuru, maana nina watu wengi
katika mji huu”. 11 Paulo akakaa huko kwa muda wa mwaka mmoja na miezi sita
akifundisha neno la Mungu miongoni mwao. 12 Lakini Galio alipofanywa mtawala
wa Akaya, Wayahudi walisimama pamoja kinyume na Paulo na kumpeleka mbele ya
kiti cha hukumu, 13 wakisema, “Mtu huyu huwashawishi watu wamwabudu Mungu
kinyume cha sheria”. 14 Wakati Paulo alipokuwa akitaka kusema, Galio akawaambia
Wayahudi, “Ninyi Wayahudi, kama ingelikuwa ni kosa au uhalifu, ingekuwa halali
kuwashughulikia. 15 Lakini kwa sababu ni maswali, yanayohusu maneno na majina,
na sheria zenu, basi hukumuni ninyi wenyewe. Mimi sitamani kuwa hakimu
kwa habari ya mambo hayo.” 16 Galio akawaamuru waondoke mbele ya kiti cha
hukumu, 17 Hivyo, wakamkamata Sosthene, kiongozi wa sinagogi, wakampiga mbele
ya kiti cha hukumu. Lakini Galio hakujali walichokifanya. 18 Paulo, baada ya
kukaa pale kwa muda mrefu, aliwaacha ndugu na kwenda kwa meli Siria pamoja
na Prisila na Akwila. Kabla ya kuondoka bandarini, alinyoa nywele zake kwani
alikuwa ameapa kuwa Mnadhiri. 19 Walipofika Efeso, Paulo alimwacha Prisila na

Akwila pale, lakini yeye mwenyewe akaingia kwenye sinagogi na kujadiliana na
Wayahudi. 20 Walipomwambia Paulo akae nao kwa muda mrefu, yeye alikataa.
21 Lakini akaondoka kwao, akawaambia, “Nitarudi tena kwenu, ikiwa ni mapenzi
ya Mungu”. Baada ya hapo, akaondoka kwa meli kutoka Efeso. 22 Paulo alipotua
Kaisaria, alipanda kwenda kusalimia Kanisa la Yerusalemu, kisha akashuka chini
kwa kanisa la Antiokia. 23 Baada ya kukaa kwa muda pale, Paulo aliondoka kupitia
maeneo ya Galatia na Frigia na kuwatia moyo wanafunzi wote. 24 Myahudi mmoja
aitwaye Apolo, aliyezaliwa huko Alexandria, alikuja Efeso. Alikuwa na ufasaha
katika kuongea na hodari katika Maandiko. 25 Apollo alikuwa ameelekezwa katika
mafundisho ya Bwana. Kwa jinsi alivyokuwa na bidii katika roho, aliongea na
kufundisha kwa usahihi mambo yanayomuhusu Yesu, ila alijua tu ubatizo wa Yohana.
26 Apolo akaanza kuzungumza kwa ujasiri katika hekalu. Lakini Prisila na Akwila
walipomsikia, walifanya urafiki naye na wakamwelezea juu ya njia za Mungu
kwa usahihi. 27 Alipotamani kuondoka kwenda Akaya, ndugu walimtia moyo na
kuwaandikia barua wanafunzi walioko Akaya ili wapate kumpokea. Alipowasili,
kwa neema aliwasaidia sana wale waliomini. 28 Kwa nguvu zake na maarifa, Apolo
aliwazidi Wayahudi hadharani akionesha kupitia maandiko ya kuwa Yesu ndiye
Kristo.

# 19

1 Ikawa kwamba Apolo alipokuwa Korintho, Paulo akapita nyanda za juu na kufika
katika mji wa Efeso, na akakuta wanafunzi kadhaa huko. 2 Paulo akawaambia,
“Je, mlipokea Roho Mtakatifu mlipoamini?” Wakamwambia, “Hapana, hatukuweza
hata kusikia kuhusu Roho Mtakatifu.” 3 Paul alisema, “Sasa ninyi mlibatizwaje?”
Wakasema, “Katika ubatizo wa Yohana. 4 Basi Paulo akajibu, “Yohana alibatiza
kwa ubatizo wa toba. Akawaambia wale watu kwamba wanapaswa kumwamini
yule ambaye angekuja baada yake, yaani, Yesu.” 5 Watu waliposikia habari hii,
wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu. 6 Na ikawa Paulo alipoweka mikono yake
juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao na wakaanza kunena kwa lugha na kutabiri.
7 Jumla yao walikuwa wanaume wapatao kumi na wawili. 8 Paulo alienda katika
sinagogi akanena kwa ujasiri kwa muda wa miezi mitatu. Alikuwa akiongoza
majadiliano na kuwavuta watu kuhusu mambo yanayohusu ufalme wa Mungu.
9 Lakini Wayahudi wengine walikuwa wakaidi na wasiotii, walianza kusema mabaya
kuhusu njia ya Kristo mbele ya umati. Basi Paulo aliachana nao na akawatenga
waaminio mbali nao. Naye alianza kuongea kila siku katika ukumbi wa Tirano.
10 Hii iliendelea kwa miaka miwili, kwa hiyo wote waliokuwa wanaishi katika Asia
walisikia neno la Bwana, wote Wayahudi na Wayunani. 11 Mungu alikuwa akifanya
matendo makuu kwa mikono ya Paulo, 12 kwamba hata wagonjwa waliponywa, na
roho chafu waliwatoka, wakati walipochukua leso na nguo zilizotoka mwilini mwa
Paulo. 13 Lakini palikuwapo Wayahudi wapunga pepo wakisafiri kupitia eneo hilo,
wakilitumia jina la Yesu kwa ajili ya matumizi yao wenyewe. Wakiwaambia wale
walikuwa na pepo wachafu; Wakisema, “Ninawaamuru mtoke kwa jina la Yesu
ambaye Paulo anamhubiri.” 14 Waliofanya haya walikuwa wana saba wa kuhani
Mkuu wa Kiyahudi, Skewa. 15 Roho wachafu wakawajibu, “Yesu namjua, na Paulo
namjua; lakini ninyi ni nani? “ 16 Yule roho mchafu ndani ya mtu akawarukia
wapunga pepo na akawashinda nguvu na kuwapiga. Ndipo wakakimbia kutoka ile
nyumba wakiwa uchi na kujeruhiwa. 17 Jambo hili likajulikana kwa wote, Wayahudi
na Wayunani, ambao waliishi huko Efeso. Wakawa na hofu sana, na jina la Bwana
likazidi kuheshimiwa. 18 Pia, wengi wa waumini walikuja na wakaungama na
wakidhihirisha matendo mabaya waliyoyafanya. 19 Wengi waliokuwa wakifanya

uganga wakakusanya vitabu vyao, wakavichoma mbele ya kila mtu. Wakati wao
walipohesabu thamani ya vitu hivyo, ilikuwa vipande hamsini elfu vya fedha.
20 Hivyo Neno la Bwana likaenea kwa upana sana katika nguvu. 21 ya Paulo
kukamilisha huduma yake kule Efeso, Roho akamwongoza kwenda Yerusalemu
kupitia Makedonia na Akaya; Akasema, "Baada ya kuwako huko, yanipasa kuiona
Rumi pia." 22 Paul akawatuma Makedonia wanafunzi wake wawili, Timotheo na
Erasto, ambao walikuwa wamemsaidia. Lakini yeye mwenyewe akabaki Asia kwa
muda. 23 Wakati huo kulitokea ghasia kubwa huko Efeso kuhusu ile Njia. 24 Sonara
mmoja jina lake Demetrio, ambaye aliyetengeneza visanamu vya fedha vya mungu
Diana, alileta biashara kubwa kwa mafundi. 25 Hivyo akawakusanya mafundi wa kazi
hiyo na kusema, "Waheshimiwa, mnajua kwamba katika biashara hii sisi tunaingiza
pesa nyingi. 26 Mnaona na kusikia kwamba, si tu hapa Efeso, bali karibia Asia yote,
huyu Paulo amewashawishi na kuwageuza watu wengi. Anasema kwamba hakuna
miungu ambayo imefanywa kwa mikono. 27 Na si tu iko hatari kwamba biashara
yetu itakuwa haihitajiki tena, lakini pia na hekalu la mungu mke aliye mkuu Diana
anaweza kuchukuliwa kuwa hana maana. Tena angeweza hata kupoteza ukuu wake,
yeye ambaye Asia na dunia humwabudu." 28 Waliposikia haya, walijawa na hasira
na wakapiga kelele, wakisema, "Diana wa Waefeso ni mkuu." 29 Mji wote ukajaa
ghasia, na watu wakakimbia pamoja ndani ya ukumbi wa michezo. wakawakamata
wasafiri wenzake na Paulo, Gayo na Aristariko, waliotoka Makedonia. 30 Paulo
alitaka kuingia katika umati wa watu, lakini wanafunzi walimzuia. 31 Pia, baadhi
ya maafisa wa mkoa wa Asia ambao walikuwa marafiki zake wakampelekea ujumbe
kwa nguvu kumwomba asiingie katika ukumbi wa michezo. 32 Baadhi ya watu
walikuwa wakisema kitu hiki na wengine jambo lile, kwa sababu umati wa watu
ulikuwa umechanganyikiwa. Wengi wao hawakuweza hata kujua kwa nini walikuja
pamoja. 33 Wayahudi wakamleta Iskanda nje ya umati wa watu na kumuweka juu
mbele ya watu. Iskanda akatoa ishara kwa mkono wake kutoa maelezo kwa watu.
34 Lakini walipotambua kuwa yeye ni Myahudi, wote wakapiga kelele kwa sauti moja
kwa muda wa saa mbili, "Diana ni mkuu wa Wafeso." 35 Baada ya karani wa mji
kuunyamazisha umati, alisema, 'Enyi wanaume wa Efeso, ni nani asiyejua kwamba
mji huu wa Efeso ni mtunzaji wa hekalu la Diana mkuu na ile picha ilivyoanguka
kutoka mbinguni? 36 Kuona Basi kwamba mambo haya hayatawezekana, tunapaswa
kuwa na utulivu na msifanye chochote kwa haraka. 37 Kwa maana mmewaita
watu hawa hapa mahakamani ambao si wezi wa hekalu wala si wenye kumkufuru
mungu wetu mke. 38 Kwa hiyo, kama Demetrio na mafundi waliopamoja naye wana
mashtaka dhidi ya mtu yeyote, mahakama ziko wazi na maliwali wapo. Na waletwe
mbele ya shauri. 39 Lakini kama wewe ukitafuta chochote kuhusu mambo mengine,
yatashughurikiwa katika kikao halali. 40 Kwa kweli tuko katika hatari ya kutuhumiwa
kuhusu ghasia siku hii. Hakuna sababu ya machafuko haya, na hatutakuwa na uwezo
wa kuyaeleza. 41 Baada ya kusema haya, aliwatawanya makutano.

# 20

1 Baada ya ghasia kumalizika, Paulo aliwaita wanafunzi na kuwatia moyo. Kisha
kuwaaga na akaondoka kwenda Makedonia. 2 Naye akiishakupita mikoa hiyo na
alikuwa akiwatia moyo waamuni, akaingia Uyunani. 3 Baada ya yeye kuwa pale
kwa muda wa miezi mitatu, njama ziliundwa dhidi yake na Wayahudi alipokuwa
akikaribia kusafiri kwa njia ya bahari kuelekea Shamu, hivyo aliazimu kurudi kupitia
Makedonia. 4 Walioandamana naye hadi Asia walikuwa Sopatro, mwana wa Pirho
kutoka Berea; Aristariko na Sekundo, wote kutoka waamini wa Wathesalonike; Gayo
wa Derbe; Timotheo; Tikiko na Trofimo kutoka Asia. 5 Lakini watu hawa wamekwisha

tangulia na walikuwa wanatungojea kule Troa. 6 kwa njia ya Bahari kutoka Filipi
baada ya siku za mikate isiyotiwa chachu, na katika siku tano tukawafikia huko
Troa. Tulikaa huko kwa siku saba. 7 Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa
tumekusanyika pamoja ili kuumega mkate, Paulo alizungumza na Waamini. Alikuwa
akipanga kuondoka kesho yake, hivyo akaendelea kuongea hadi usiku wa manane.
8 Kulikuwa na taa nyingi katika chumba cha juu ambapo tulikuwa tumekusanyika
pamoja. 9 Katika dirisha alikuwa amekaa kijana mmoja jina lake Utiko, ambaye
alielemewa na usingizi mzito. Hata Paulo alipokuwa akihutubu kwa muda mrefu,
kijana huyu, akiwa amelala, akaanguka chini kutoka ghorofa ya tatu na aliokotwa
akiwa amekufa. 10 Lakini Paulo alishuka chini, alijinyoosha yeye mwenyewe juu
yake, akamkumbatia. Kisha akasema, “Msikate tamaa, kwa kuwa yu hai.” 11 Kisha
akapanda tena ghorofani na akaumega mkate, akala. Baada ya kuzungumza nao
kwa muda mrefu hadi alfajiri, akaondoka. 12 Wakamleta yule kijana akiwa hai
wakafarijika sana. 13 Sisi wenyewe tulitangulia mbele ya Paul kwa meli na tukaelekea
Aso, ambapo sisi tulipanga kumchukua Paul huko. Hiki ndicho yeye mwenyewe
alitaka kufanya, kwa sababu alipanga kwenda kupitia nchi kavu. 14 Alipotufikia huko
Aso, tukampakia kwenye Meli tukaenda Mitilene. 15 Kisha sisi tukatweka kutoka huko
na siku ya pili tulifika upande wa pili wa kisiwa cha Kio. Siku iliyofuata, tukawasili
kisiwa cha Samo, na kesho yake tukafika mji wa Mileto. 16 Kwa sababu Paulo alikuwa
ameamua kusafiri kupitia Efeso, ili kwamba asitumie muda wowote katika Asia; kwa
maana alikuwa na haraka ya kuwahi Yerusalemu kwa ajili ya sikukuu ya Pentekoste,
kama ingeliwezekana yeye kufanya hivyo. 17 Kutoka Mileto akatuma watu hadi Efeso
na akawaita wazee wa Kanisa. 18 Walipofika kwake, akawaambia, ninyi wenyewe
mwajua tangu siku ya kwanza nilipokanyaga hapa Asia, jinsi nilivyokuwa kwenu
muda wote. 19 Nimemtumikia Bwana kwa unyenyekevu wote na kwa machozi,
na mateso yaliyonipata mimi kwa hila za Wayahudi. 20 Mwajua jinsi ambavyo
sikujizuia kutangaza kwenu kitu chochote ambacho kilikuwa muhimu, na jinsi mimi
nilivyowafundisha wazi wazi na pia kwenda nyumba kwa nyumba. 21 Mnajua jinsi
mimi nilivyoendelea kuwaonya Wayahudi na Wayunani juu ya toba kwa Mungu na
imani katika Bwana wetu Yesu. 22 Na sasa, angalieni, mimi, nikiwa ninamtii Roho
Mtakatifu kuelekea Yerusalemu, nisiyajue mambo ambayo yatanitokea mimi huko,
23 ila kwa kuwa Roho Mtakatifu hunishuhudia mimi katika kila mji na anasema
kwamba minyororo na mateso ndivyo vinavyoningojea. 24 Lakini mimi si kufikiria
kwamba maisha yangu ni kwa njia yoyote ya thamani kwangu, ili niweze kumaliza
mwendo wangu na huduma niliyopokea kutoka kwa Bwana Yesu, kuishuhudia injili
ya neema ya Mungu. 25 Na sasa, tazama, najua kwamba wote, miongoni mwa wale
nilioenda kuwahubiri Ufalme, hamtaniona uso tena. 26 Kwa hiyo nawashuhudia
leo hii, kwamba sina hatia kwa damu ya mtu yeyote. 27 Kwa maana sikujizuia
kuwatangazia mapenzi yote ya Mungu. 28 Kwa hiyo iweni waangalifu juu yenu ninyi
wenyewe, na juu ya kundi lolote ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa
waangalizi. Iweni waangalifu kulichunga kusanyiko la Bwana, ambalo alilinunua
kwa damu yake mwenyewe. 29 Najua kwamba baada ya kuondoka kwangu, mbwa
mwitu wakali wataingia kwenu, na wasilihurumie kundi. 30 Najua kwamba hata
miongoni mwenu wenyewe baadhi ya watu watakuja na kusema mambo mapotovu,
ili kuwavuta wanafunzi wawafuate wao. 31 Kwa hiyo muwe macho. Kumbukeni
kwamba kwa miaka mitatu sikuweza kuacha kuwafundisha kila mmoja wenu kwa
machozi usiku na mchana. 32 Na sasa mimi nawakabidhi kwa Mungu, na kwa
neno la neema yake, ambalo laweza kuwajenga na kuwapa urithi pamoja nao
wote waliowekwa wakfu kwa Mungu. 33 Sikutamani fedha, dhahabu, au mavazi.
34 Mnajua ninyi wenyewe kwamba mikono hii imenipatia mahitaji yangu mwenyewe

na mahitaji ya wale waliokuwa pamoja nami. 35 Katika mambo yote niliwapa mfano
wa jinsi inavyopasa kuwasaidia wanyonge kwa kufanya kazi, na jinsi mnavyopaswa
kukumbuka maneno ya Bwana Yesu, maneno ambayo yeye mwenyewe alisema: "Ni
heri kutoa kuliko kupokea." 36 Baada ya kusema namna hii, alipiga magoti akaomba
pamoja nao. 37 Wote wakalia sana na kumwangukia Paulo shingoni na kumbusu.
38 Walihuzunika zaidi ya yote kwa sababu ya kile ambacho alikuwa amesema,
kwamba kamwe hawatauona uso wake tena. Kisha wakamsindikiza merikebuni.

# 21

1 Wakati tulipokua tumeachana nao, na tunasafiri baharini, tukafika moja kwa
moja kwenye mji wa Kosi, na kesho yake tukafika mji wa Rodo, na kutoka huko
tukafika mji wa Patara. 2 Tulipopata meli inayovuka kwenda Foinike, tulipanda
tukasafiri. 3 Tulipofika mbele ya kisiwa cha Kipro, tukaiacha upande wa kushoto,
tukasafiri hadi Siria, tukaweka nanga katika mji wa Tiro, kwa sababu huko ndiko
meli ilikuwa ipakuliwe shehena yake. 4 Baada ya kuwaona wanafunzi, tukakaa
huko siku saba. Wanafunzi hawa wakamwambia Paulo kupitia kwa Roho kwamba
yeye asikanyage Yerusalemu. 5 Hata tulipotimiza siku zile, sisi tukaondoka tukaenda
zetu. Wote pamoja, na wanawake zao na watoto wao, walitusindikiza katika njia
zetu hadi tulipotoka nje ya mji. Kisha tukapiga magoti pwani, tukaomba, tukaagana
kila mmoja. 6 Tukapanda meli, huku nao wakarudi nyumbani kwao tena. 7 Hata
tulipomaliza safari yetu kutoka Tiro, tukafika Tolemai. Pale tulisalimia ndugu, na
kukakaa nao kwa siku moja. 8 Kesho yake tuliondoka tukaenda Kaisaria. Sisi
tukaingia nyumbani mwa Filipo, mhubiri wa injili, aliyekuwa mmoja wa wale saba,
nasi tukakaa pamoja naye. 9 Mtu huyu alikuwa na mabinti wanne mabikira ambao
walitabiri. 10 Baada ya kukaa huko kwa siku kadhaa, akashuka kutoka Uyahudi nabii
mmoja aitwaye Agabo. 11 Yeye alikuja kwetu na akautwaa mkanda wa Paulo. kwa
huo alijifunga miguu na mikono yake mwenyewe na kusema, "Roho Mtakatifu asema
hivi," "Wayahudi wa Yerusalemu watamfunga mtu anayemiliki mkanda huu, nao
watamkabidhi mikononi mwa watu wa mataifa." 12 Tuliposikia mambo hayo, sisi na
watu waliokuwa wakiishi mahali pale tulimsihi Paulo asipande kwende Yerusalemu.
13 Ndipo Paulo alijibu, "Mnafanya nini, mnalia na kunivunja moyo wangu? Kwa
maana niko tayari, siyo tu kufungwa, lakini pia kufia huko Yerusalemu kwa ajili ya
jina la Bwana Yesu." 14 Kwa vile Paulo hakutaka kushawishiwa, tuliacha na kusema,
" Basi mapenzi ya Bwana yafanyike." 15 Baada ya siku hizi, tulichukua mifuko yetu
na tukapanda Yerusalemu. 16 Baadhi ya wanafunzi kutoka Kaisaria pia walifuatana
nasi. Wakamleta mtu mmoja aitwaye Mnasoni, mtu wa Kipro, mwanafunzi wa
zamani, ambaye tulikaa naye. 17 Tulipofika Yerusalemu, ndugu walitukaribisha
kwa furaha. 18 Kesho yake Paulo aliendа pamoja nasi kwa Yakobo, na wazee wote
walikuwepo. 19 Baada ya kuwasalimu, aliwapa taarifa moja baada ya nyingine ya
mambo ambayo Mungu aliyotenda miongoni mwa mataifa kwa kupitia huduma yake.
20 Wakati waliposikia hayo, wakamsifu Mungu, na wakamwambia, "Unaona, ndugu,
kuna maelfu wangapi wameamini miongoni mwa Wayahudi. Wao wote wana nia
ya kushika sheria. 21 Wameambiwa kuhusu wewe, kwamba unafundisha Wayahudi
wanaoishi kati ya mataifa kuachana na Musa, na kwamba unawaambia wasiwatahiri
watoto wao, na wasifuate desturi za zamani. 22 Tunapaswa tufanye nini? Bila
shaka watasikia kwamba wewe umekuja. 23 Hivyo fanya kile sisi tunachokuambia
sasa: tunao watu wanne ambao wameweka nadhiri. 24 Wachukue watu hawa na
ujitakase mwenyewe pamoja nao, na uwalipie gharama zao, ili waweze kunyoa
vichwa vyao. Hivyo kila mmoja apate kujua kwamba mambo waliyoambiwa kuhusu
wewe ni ya uongo. Watajifunza kwamba wewe pia unafuata sheria. 25 Lakini

kwa habari za mataifa ambao wamekuwa waumini, tuliandika na kutoa maagizo
kwamba wanapaswa kujiepusha na vitu vilivyotolewa dhabihu kwa sanamu, na
damu, kutokana na kile kilichonyongwa, na wajiepushe na uasherati.” 26 Ndipo,
Paulo aliwatwaa wanaume, na siku ya pili, akajitakasa mwenyewe pamoja nao,
akaingia Hekaluni, kutangaza kipindi cha siku za kujitakasa, hadi sadaka itolewa
kwa ajili ya kila mmoja wao. 27 Siku hizo saba zilipokaribia kumalizika, baadhi ya
Wayahudi kutoka Asia wakamuona Paulo Hekaluni, na makutano wakakasirika, na
wakamnyoshea mikono. 28 Walikuwa wanapiga kelele, “Watu wa Israeli, tusaidieni.
Huyu ni yule mtu anayewafundisha watu kila mahali mambo ambayo ni kinyume na
watu, sheria, na mahali hapa. Pia amewaleta Wayunani katika Hekalu na kupanajisi
mahali hapa patakatifu.” 29 Kwa kuwa mwanzoni walikuwa wamemwona Trofimo
Muefeso akiwa pamoja naye mjini, nao walidhani kwamba Paulo alimleta hekaluni.
30 Mji wote ulikuwa na taharuki, na watu wakakimbia pamoja na kumkamata Paulo.
Wakamtoa nje ya Hekalu, na milango mara ikafungwa. 31 Walipokuwa wakijaribu
kumuua, habari zilimfikia mkuu wa jeshi la walinzi kuwa Yerusalemu yote ilikuwa
imejaa ghasia. 32 Mara hiyo akawachukua askari na jemadari akaukimbilia umati.
Wakati Watu walipomwona mkuu wa jeshi na askari, wakaacha kumpiga Paulo.
33 Kisha mkuu wa jeshi alimkaribia na akamshika Paulo, na akaamuru afungwe
minyororo miwili. Akamuuliza yeye ni nani na amefanya nini. 34 Baadhi ya watu
kwenye umati walikuwa wanapayuka kitu hiki na wengine kingine. Kwa kuwa
jemadari hakuweza kuwaambia chochote kwa sababu ya zile kelele, akaamuru Paulo
aletwe ndani ya ngome. 35 Basi alipofika kwenye ngazi, akachukuliwa na askari kwa
sababu ya ghasia za umati. 36 Maana umati wa watu walimfuata na waliendelea
kupiga kelele, “Mwondoeni huyu!” 37 Paulo alipokuwa analetwa ndani ya ngome,
alimwambia mkuu wa jeshi, “Naweza kukwambia kitu?” Yule mkuu wa jeshi
akasema, “Je unaongea Kiyunani? 38 Je, wewe si yule Mmisri ambaye awali aliongoza
uasi na alichukua magaidi elfu nne nyikani?” 39 Paulo akasema, “Mimi ni Myahudi,
kutoka mji wa Tarso ya Kilikia. Mimi ni raia wa mji maarufu. Nawaomba, mniruhusu
nizungumze na watu.” 40 Wakati jemadari alipompa ruhusa, Paulo akasimama penye
ngazi na akatoa ishara kwa watu kwa mkono wake. Wakati kulipokuwa na ukimya
sana, akaongea nao kwa Kihebrania. Akasema,

# 22

1 “Ndugu na baba zangu, sikilizeni utetezi wangu nitakaofanya kwenu sasa.”
2 Makutano walipo sikia Paulo akiongea nao kwa kiebrania, wakanyamaza. Akasema,
3 “Mimi ni myahudi, nimezaliwa mji wa Tarso eneo la Kilikia, ila nilipata elimu katika
mji huu, miguuni pa Gamalieli. Nilifundishwa kulingana na njia sahihi za sheria za
baba zetu. Mimi ninabidii ya Mungu, kama ninyi nyote mlivyo leo. 4 Niliwatesa
kwa njia hii hadi kufa; nikawafunga wanaume na wanawake na kuwatupa gerezani.
5 Hata kuhani mkuu na wazee wote wanaweza kutoa ushahidi kwamba nilipokea
barua kutoka kwao kwa ajili ya ndugu walio Dameski, kwangu mimi kusafiri kwenda
huko. Ilikuwa niwalete watu Yerusalemu wa njia ile ili wafungwe na kuadhibiwa.
6 Ilitokea kwamba pale nilipokua nikisafiri nakaribia Dameski, majira ya mchana
ghafla nuru kuu ikatokea mbinguni ikaanza kuniangaza. 7 Nikaanguka chini na
kusikia sauti ikiniambia, 'Sauli, Sauli kwanini unaniudhi?' 8 Nikajibu, 'wewe ni nani,
Bwana?' Akaniambia, 'Mini ni Yesu Mnazareti, ambaye wewe unaniudhi.' 9 Wale
waliokuwa na mimi waliiona nuru, ila hawakusikia sauti ya yule alie ongea na
mimi. 10 Nikasema, 'Nifanye nini, Bwana?' Bwana akaniambia, 'Simama na uingie
Dameski; huko utaambiwa kila kitu unachopaswa kufanya.' 11 Sikuweza kuona kwa
sababu ya muangaza wa nuru ile, ndipo nikaenda Dameski kwa kuongozwa na

mikono ya wale waliokuwa na mimi. 12 Huko nikakutana na mtu aitwaye Anania,
alikuwa mtu aliyeshika sheria na mwenye kuheshimika mbele ya Wayahudi wote
walioishi huko. 13 Akaja kwangu, akasimama mbele yangu, na kusema, 'Ndugu yangu
Sauli, upate kuona.'Kwa muda ule ule nikamuona. 14 Akasema, 'Mungu wa baba
zetu amekuchagua wewe upate kujua mapenzi yake, kumuona yule mwenyehaki,
na kusikia sauti itokayo kwenye kinywa chake. 15 Kwa sababu utakuwa shahidi
kwake kwa watu wote juu ya uliyoyaona na kusikia. 16 Basi sasa kwa nini
unasubiri? Amka, ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliita jina lake.' 17 Baada
ya kurejea Yerusalemu, na nilipokuwa nikisali ndani ya hekalu, ikatokea kwamba
nikapewa maono. 18 Nikamuona akiniambia, 'Hima na utoke Yerusalemu haraka,
kwa sababu hawatakubali ushuhuda wako kuhusu mimi.' 19 Nikasema, 'Bwana, wao
wenyewe wanajua niliwafunga gerezani na kuwapiga wale waliokuamini katika kila
sinagogi. 20 Na damu ya Stefano shahidi wako ilipomwagwa, Mimi pia nilikuwa
nimesimama karibu na kukubali na nilikuwa nalinda nguo za wale waliomwua.'
21 Lakini aliniambia, 'Enenda, kwa sababu mimi nitakutuma uende mbali kwa watu
wa mataifa."' 22 Watu wakamruhusu aongee juu ya neno hili. Lakini baadaye
walipaza sauti na kusema, "mwondoe mtu huyu katika nchi: kwa sababu sio sahihi
aishi." 23 Walipokuwa wakipaza sauti, na kutupa mavazi yao na kutupa mavumbi
juu, 24 jemedari mkuu akaamuru Paulo aletwe ngomeni. Akaamuru aulizwe huku
anapigwa mijeledi, ili yeye mwenyewe ajue kwa nini walikuwa wanampigia kelele
namna ile. 25 Hata walipokuwa wamemfunga kwa kamba, Paulo akamwambia yule
akida aliye simama karibu naye, "Je! ni haki kwenu kumpiga mtu aliye Mrumi
na bado hajahukumiwa?" 26 Yule akida aliposikia maneno haya, akaenda kwa
jemedari mkuu na kumwambia, akisema, "Unataka kufanya nini? Kwa maana mtu
huyu ni mrumi." 27 Jemedari mkuu akaja na kumwambia, "Niambie, je wewe ni
raia wa Rumi?" Paulo akasema, "Ndiyo." 28 Jemedari akamjibu, "Ni kupitia kiasi
kikubwa cha pesa ndipo nilipata uraia." Lakini Paulo akamwambia, "Mimi ni mrumi
wa kuzaliwa." 29 Basi wale waliokuwa tayari kwenda kumuuliza wakaondoka na
kumwacha wakati huo huo. Na jemedari naye akaogopa, alipojua kuwa Paulo ni
Mrumi, na kwa sababu amemfunga. 30 Siku iliyofuatayo, jemedari mkuu alitaka
kujua ukweli kuhusu mashtaka ya Wayahudi dhidi ya Paulo. Hivyo akamfungua
vifungo vyake akaamuru wakuu wa makuhani na baraza lote wakutane. Akamleta
Paulo chini, na kumweka katikati yao.

# 23

1 Paulo akawaangalia moja kwa moja watu wa baraza na kusema, "Ndugu zangu,
nimeishi mbele za Mungu kwa dhamira nzuri hadi hivi leo." 2 Kuhani mkuu
Anania akawaamuru wale waliosimama karibu naye wampige kinywa chake. 3 Ndipo
Paulo akamwambia, "Mungu atakupiga wewe, ukuta uliopakwa chokaa. Umekaa
ukinihukumu kwa sheria, nawe unaamuru nipigwe kinyume cha sheria?" 4 Wale
waliokuwa wamesimama karibu naye wakasema, "Hivi ndivyo unavyomtukana
kuhani mkuu wa Mungu?" 5 Paulo akasema, "ndugu zangu, mimi sikujua kwamba
huyu ni kuhani mkuu. Kwa kuwa imeandikwa, hutazungumza vibaya juu ya
mtawala wa watu wako." 6 Paulo alipoona ya kwamba upande mmoja wa baraza
ni Masadukayo na wengine Mafarisayo, akapaza sauti na kusema, "ndugu zangu,
mimi ni Mfarisayo, mwana wa Mfarisayo. Ni kwa sababu hii nategemea kwa ujasiri
ufufuo wa wafu ninao hukumiwa nao." 7 Alipoyasema haya, malumbano makubwa
yakatokea baina ya Mafarisayo na Masadukayo, na mkutano ukagawanyika. 8 Kwani
Masadukayo husema hakuna ufufuo, malaika wala hakuna roho, ila Mafarisayo
husema haya yote yapo. 9 Ghasia kubwa ikatokea na baadhi ya waandishi

waliokuwa upande wa Mafarisayo wakasimama na kujadili, wakisema, “hatujaona
chochote kibaya dhidi ya mtu huyu. Vipi kama roho au malaika ameongea na
yeye?” 10 Wakati kulitokea hoja kubwa, mkuu wa majeshi aliogopa kwamba Paulo
angeraruliwa vipande vipande na wao, hivyo akaamuru wanajeshi washuke chini
na kumchukua kwa nguvu kutoka kwa wajumbe wa baraza, na kumleta katika
ngome. 11 Usiku uliofuata Bwana alisimama karibu naye na kusema, “Usiogope,
kwa kuwa umenishuhudia katika Yerusalemu, hivyo utatoa ushahidi pia katika
Roma.” 12 Kulipokucha, baadhi ya Wayahudi walifanya agano na kuita laana juu
yao wenyewe: walisema ya kwamba hawatakula wala kunywa chochote mpaka
watakapomuua Paulo. 13 Kulikuwa na watu zaidi ya arobaini ambao walifanya njama
hii. 14 wakaenda kwa wakuu wa makuhani na wazee na kusema, “Tumejiweka
wenyewe kwenye laana kuu, tusile chochote hadi tutakapomwua Paulo. 15 Hivyo
sasa, baraza limwambie jemadari mkuu amlete kwenu, kana kwamba mnaamua kesi
yake kwa usahihi. Kwetu sisi tuko tayari kumwua kabla hajaja hapa.” 16 Lakini
mtoto wa dada yake na Paulo akasikia kwamba kulikuwa na njama, akaenda
akaingia ndani ya ngome na kumwambia Paulo. 17 Paulo akamwita akida mmoja
akasema, “Mchukue kijana huyu kwa jemadari; maana ana neno la kumwambia.”
18 Basi akida akamchukua yule kijana akampeleka kwa jemedari mkuu akamwambia,
“Paulo yule mfungwa aliniita akataka nikuletee kijana huyu kwako. Ana neno
la kukuambia.” 19 Yule jemadari mkuu akamshika kwa mkono akajitenga naye
kando, na akamwuliza, “Ni kitu gani unachotaka kuniambia?” 20 Kijana yule
akasema, “Wayahudi wamepatana kukuomba umlete Paulo kesho kwenye baraza
kana kwamba wanataka kupata habari zake kwa usahili zaidi. 21 Basi wewe usikubali
kwa maana watu zaidi ya arobaini wanamvizia. Wamejifunga kwa laana, wasile
wala wasinywe hata watakapomwua. Hata sasa wako tayari, wakisubiria kibali
toka kwako.” 22 Basi yule jemadari mkuu akamwacha kijana aende zake, baada ya
kumwagiza “usimwambie mtu yeyote ya kwamba umeniarifu haya.” 23 Akawaita
maakida wawili akasema watayarisheni askari mia mbili kwenda Kaisaria na askari
wapanda farasi sabini, na wenye mikuki mia mbili, mtaondoka zamu ya tatu ya usiku.
24 Akawaambia kuweka wanyama tayari ambaye Paulo atamtumia na kumchukua
salama kwa Feliki Gavana. 25 Akaandika barua kwa namna hii, 26 Klaudio Lisia
kwa Liwali mtukufu Feliki, salamu. 27 Mtu huyu alikamatwa na wayahudi wakawa
karibu kumwua, ndipo nikaenda pamoja na kikosi cha askari nikamwokoa, nilipopata
habari ya kuwa yeye ni raia wa kirumi. 28 Nilitaka kujua kwa nini wamemshtaki,
hivyo nikampeleka kwenye baraza. 29 Nikaona kwamba alikuwa ameshitakiwa
kwa ajili ya maswali ya sheria yao, wala hakushitakiwa neno lolote la kustahili
kuuawa wala kufungwa. 30 Kisha ikajulikana kwangu kwamba kuna njama dhidi
yake, hivyo kwa haraka nikamtuma kwako, na kuwaagiza wanaomshitaki pia walete
mashitaka dhidi yake mbele yako. Wakaagana.” 31 Basi wale askari wakatii amri:
wakamchukua Paulo wakampeleka hata Antipatri usiku. 32 Siku iliyofuata, maaskari
wengi wakawaacha wale wapanda farasi waende pamoja naye, nao wakarudi zao
ngomeni. 33 Na wapanda farasi walipofika Kaisaria, na kumpa liwali ile barua,
wakamweka Paulo mbele yake. 34 Naye liwali alipoisoma barua, alimuuliza Paulo
alitokea jimbo gani; alipojua ya kwamba ni mtu wa Kilikia, 35 akasema, “Nitakusikia
wewe watakapo kuja wale waliokushitaki,” akaamuru awekwe katika ikulu ya
Herode.

# 24

1 Baada ya siku tano, Anania kuhani mkuu, baadhi ya wazee na msemaji mmoja
aitwaye Tertulo, wakaenda pale. Watu hawa wameleta mashtaka dhidi ya Paulo

kwa gavana. 2 Paulo alipo simama mbele ya gavana, Tertulo akaanza kumshitaki
na kusema kwa gavana, “kwa sababu yako tuna amani kuu; na kwa maono yako
yanaleta mageuzi mazuri katika taifa letu; 3 basi kwa shukurani yote tunapokea
kila kitu ukifanyacho, Wasalam mheshimiwa Feliki. 4 Lakini nisikuchoshe zaidi,
nakusihi unisikilize maneno machache kwa fadhili zako. 5 Kwa maana tumempata
mtu huyu mkorofi, na anasababisha Wayahudi wote kuasi duniani. Tena ni kiongozi
wa madhehebu ya Wanazorayo. (Zingatia: Sehemu ya maneno ya mstari huu 24: 6
6 Na tena alijaribu kulitia hekalu unajisi hivyo tukamkamata., haumo kwenye nakala
bora za kale). (Zingatia: Mstari huu 7 Lisiasi, afisa, alikuja na akamchukua kwa nguvu
mikononi mwetu., haumo kwenye nakala bora za maandiko ya kale). 8 Ukimwuliza
Paulo kuhusu mambo haya, hata utaweza kujifunza ni kitu gani tumemshtakia.”
9 Wayahudi nao wakamshtaki Paulo, wakisema kwamba haya mambo yalikuwa
kweli. 10 Liwali alipompungia mkono ili Paulo aongee, Paulo alijibu, “Ninajua ya
kwamba kwa miaka mingi umekua mwamuzi wa taifa hili, na nina furaha kujieleza
mwenyewe kwako. 11 Waweza kuhakikisha kuwa hazijapita siku zaidi ya kumi na
mbili tangu nilipopanda kwenda kuabudu Yerusalemu. 12 Na waliponikuta katika
hekalu, sikubishana na mtu yeyote, na sikufanya fujo katika mkutano, wala katika
masinagogi wala ndani ya mji; 13 na wala hawawezi kuhakikisha kwako mashitaka
wanayoyashitaki dhidi yangu. 14 Ila nakiri hili kwako, ya kwamba kwa njia ile
ambayo wanaiita dhehebu, kwa njia iyo hiyo ninamtumikia Mungu wa baba zetu.
Mimi ni mwaminifu kwa yote yaliyoko kwenye sheria na maandiko ya manabii.
15 Nina ujasiri ule ule kwa Mungu ambao hata hao nao wanaungojea, kuja kwa ufufuo
wa wafu, kwa wote wenye haki na wasio na haki pia; 16 na kwa hili, ninafanya kazi
ili niwe na dhamira isiyo na hatia mbele za Mungu na mbele ya watu kupitia mambo
yote. 17 Sasa Baada ya miaka mingi nimekuja kuleta msaada kwa taifa langu na
zawadi ya fedha. 18 Nilipofanya hivi, Wayahudi fulani wa Asia wakanikuta ndani ya
sherehe ya utakaso ndani ya hekalu, bila kundi la watu wala ghasia. 19 Watu hawa
ambao imewapasa kuwapo mbele yako sasa hivi na waseme kile walichonacho juu
yangu kama wana neno lo lote. 20 Au watu hawa wenyewe na waseme ni kosa gani
waliloliona kwangu niliposimama mbele za baraza la kiyahudi; 21 isipokuwa kwa ajili
ya kitu kimoja nilichokisema kwa sauti niliposimama katikati yao, ' ni kwa sababu ya
ufufuo wa wafu ninyi mnanihukumu.”' 22 Feliki alikuwa ametaarifiwa vizuri kuhusu
njia, na akauahirisha mkutano. Akasema, “Lisia jemedari atakapokuja chini kutoka
Yerusalemu nitatoa maamuzi dhidi ya mashitaka yenu.” 23 Ndipo akamwamuru akida
amlinde Paulo, ila awe na nafasi na hata asiwepo mtu wakuwakataza marafiki zake
wasimsaidie wala wasimtembelee. 24 Baada ya siku kadhaa, Feliki akarudi na Drusila
mkewe aliyekuwa Myahudi, akatuma kumwita Paulo na akasikiliza toka kwake
habari za imani ndani ya Kristo Yesu. 25 Ila Paulo alipokuwa akijadiliana naye kuhusu
haki, kuwa na kiasi na hukumu itakayokuja, Feliki akapata hofu akajibu, “nenda
mbali kwa sasa, ila nikipata muda tena, nitakuita.” 26 Muda uo huo, alitegemea
kwamba Paulo atampa fedha kwa hiyo alimwita mara nyingi akaongea naye. 27 Ila
miaka miwili ilipopita, Porkio Festo akawa Liwali baada ya Feliki, ila Feliki alitaka
kujipendekeza kwa Wayahudi, hivyo akamwacha Paulo chini ya uangalizi.

# 25

1 Ndipo Festo alipoingia katika jimbo hilo na baada ya siku tatu alienda toka
Kaisaria hadi Yerusalemu. 2 Kuhani mkuu na Wayahudi mashuhuri walileta shutuma
dhidi ya Paulo kwa Festo, na walizungumza kwa nguvu kwa Festo. 3 Na walimwomba
Festo fadhili juu ya habari za Paulo apate kumwita Yerusalemu ili waweze kumwua
njiani. 4 Lakini Festo alijibu kwamba Paulo alikuwa mfungwa katika Kaisaria, na

kwamba yeye mwenyewe atarudi huko haraka. 5 Alisema “Kwa hiyo, wale ambao
wanaweza, wanaweza kwenda huko na sisi. Kama kuna kitu kibaya kwa mtu huyu,
mnapaswa kumshtaki.” 6 Baada ya kukaa siku nane au kumi zaidi, akarudi Kaisaria.
Na siku iliyofuata akakaa katika kiti cha hukumu na kuamuru Paulo aletwe kwake.
7 Alipofika, Wayahudi kutoka Yerusalemu wakasimama karibu, Wakatoa mashtaka
mengi mazito ambayo hawakuweza kuyathibitisha. 8 Paulo alijitetea na kusema, 'Si
dhidi ya jina la Wayahudi, si juu ya hekalu, na si juu ya Kaisari, nimefanya mabaya.'
9 Lakini Festo alitaka kujipendekeza kwa Wayahudi, na hivyo akamjibu Paulo kwa
kusema, 'Je, unataka kwenda Yerusalemu na kuhukumiwa na mimi kuhusu mambo
haya huko?' 10 Paulo alisema, 'ninasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kaisari
ambapo napaswa kuhukumiwa. Sijawakosea Wayahudi, kama wewe ujuavyo vema.
11 Ikiwa nimekosa na kama nimefanya kinachostahili kifo, sikatai kufa. Lakini kama
shutuma zao si kitu, hakuna mtu anaweza kunikabidhi kwao. Ninamwomba Kaisari.
' 12 Baada ya Festo kuongea na baraza akajibu, “ unamwomba Kaisari; utaenda
kwa Kaisari.” 13 Baada ya siku kadhaa, mfalme Agripa na Bernike walifika Kaisaria
kufanya ziara rasmi kwa Festo. 14 Baada ya kukaa hapo kwa siku nyingi, Festo
aliwasilisha kesi ya Paulo kwa mfalme; Akasema, 'Mtu mmoja aliachwa hapa na
Feliki kama mfungwa. 15 Nilipokuwa Yerusalemu makuhani wakuu na wazee wa
Wayahudi walileta mashtaka juu ya mtu huyu kwangu, nao waliuliza juu ya hukumu
dhidi yake. 16 Kwa hili mimi niliwajibu kwamba si desturi ya Waroma kumtoa mtu
kwa upendeleo badala yake, mtuhumiwa anapaswa kuwa na nafasi ya kuwakabili
washitaki wake na kujitetea dhidi ya tuhuma hizo. 17 Kwa hiyo, walipokuja pamoja
hapa, sikuweza kusubiri, lakini siku iliyofuata niliketi katika kiti cha hukumu na
kuamuru mtu huyo aletwe ndani. 18 Wakati washitaki waliposimama na kumshtaki,
nilifikiri kwamba hakuna mashtaka makubwa yaliyoletwa dhidi yake. 19 Badala yake,
walikuwa na mabishano fulani pamoja naye kuhusu dini yao na kuhusu Yesu ambaye
alikuwa amekufa, lakini Paulo anadai kuwa yu hai. 20 Nilikuwa nimefumbwa jinsi
ya kuchunguza suala hili, na nikamwuliza kama angeenda Yerusalemu kuhukumiwa
kuhusu mambo haya. 21 Lakini Paulo alipoitwa awekwe chini ya ulinzi kwa ajili
ya uamuzi wa Mfalme, niliamuru awekwe hata nitakapompeleka kwa Kaisari. '
22 Agripa alizungumza na Festo, “ningependa pia kumsikiliza mtu huyu.” “Festo,
akasema, “kesho utamsikiliza.” 23 Hivyo kesho yake, Agripa na Bernike walifika na
sherehe nyingi; walifika katika ukumbi na maafisa wa kijeshi, na watu mashuhuri wa
mji. Na Festo alipotoa amri, Paulo aliletwa kwao. 24 Festo akasema, “Mfalme Agripa,
na watu wote ambao wapo hapa pamoja nasi, mnamwona mtu huyu; jumuiya yote
ya Wayahudi huko Yerusalemu na hapa pia wametaka niwashauri, na wao wakapiga
kelele kwangu kwamba asiishi. 25 Naliona kwamba hakufanya lolote linalostahili
kifo; lakini kwa sababu amemwita Mfalme, niliamua kumpeleka kwake. 26 Lakini
sina kitu dhahiri cha kuandika kwa Mfalme. Kwa sababu hii, nimemleta kwako,
hasa kwako wewe, Mfalme Agripa, ili nipate kuwa na kitu cha kuandika kuhusu kesi.
27 kwa kuwa naona haina maana kumpeleka mfungwa na bila kuonyesha mashitaka
yanayomkabili.

## 26

1 Hivyo, Agripa akamwambia Paulo, `Unaruhusiwa kujitetea. ' Ndipo Paulo
akanyoosha mkono wake akajitetea hivi. 2 “Najiona mwenye furaha, Mfalme
Agripa, ili kufanya kesi yangu mbele yako leo dhidi ya mashtaka yote ya Wayahudi.
3 Hasa, kwa sababu wewe ni mtaalamu wa desturi za Wayahudi na maswali.
Hivyo naomba unisikilize kwa uvumilivu. 4 Kweli, Wayahudi wote wanajua jinsi
nilivyoishi tangu ujana wangu katika taifa langu huko Yerusalemu. 5 Wananijua

tangu mwanzo na wanapaswa kukubali kwamba niliishi kama Mfarisayo, dhehebu
lenye msimamo mkali kwenye dini yetu. 6 Sasa nimesimama hapa nihukumiwe kwa
sababu mimi naliangalia ahadi ambayo Mungu aliifanya na baba zetu. 7 Hii ni ahadi
ambayo makabila yetu kumi na mbili yanatumaini kupokea kama wakimwabudu
Mungu kwa bidii usiku na mchana. Ni kwa ajili ya tumaini hili, mfalme Agripa,
kwamba Wayahudi wananishitaki. 8 Kwa nini yeyote kati yenu anafikiri ni ajabu
kwamba Mungu hufufua wafu? 9 Wakati mmoja nilifikiria mwenyewe kwamba
ningefanya mambo mengi dhidi ya jina la Yesu wa Nazareti. 10 Nilifanya haya katika
Yerusalemu; Niliwafunga waamini wengi gerezani, na nilikuwa na mamlaka kutoka
kwa wakuu wa makuhani kufanya hivyo; na wakati wanauawa, nilipiga kura dhidi
yao. 11 Mara nyingi niliwaadhibu katika masinagogi yote na nilijaribu kuwafanya
waikane imani yao. Nilikuwa na hasira sana juu yao na niliwafukuza hata katika
miji ya ugenini. 12 Wakati nilipokuwa nikifanya haya, nilienda Dameski, nikiwa na
mamlaka na maagizo kutoka kwa makuhani wakuu; 13 nilipokuwa njiani wakati
wa mchana, Mfalme, niliona mwanga kutoka mbinguni uliokuwa mkali kuliko jua
na uling'aa kutuzunguka mimi na watu waliokuwa wakisafiri pamoja nami. 14 Sisi
sote tulipoanguka chini, nalisikia sauti ikizungumza na mimi ikisema katika lugha
ya Kiebrania: `Sauli, Sauli! Kwa nini unanitesa? Ni vigumu kwako kuupiga teke
mchokoo. 15 Ndipo nikasema, 'Wewe ni nani, Bwana?' Bwana akajibu, 'Mimi ni Yesu
ambaye unanitesa. 16 Sasa inuka usimame kwa miguu yako; sababu kwa kusudi hili
mimi nimeonekana kwako, nimekuteua kuwa mtumishi na shahidi juu ya mambo
ambayo unajua kuhusu mimi sasa na mambo nitakayokuonyesha baadaye; 17 na
Nitakuokoa kutoka kwa watu na watu wa Mataifa ambapo ninakutuma, 18 kufungua
macho yao na kuwatoa gizani kwenda kwenye mwanga na kutoka kwenye nguvu
za shetani wamgeukie Mungu; ili wapate kupokea kutoka kwa Mungu msamaha
wa dhambi na urithi ambao nimewapa wale niliowatenga kwa imani iliyo kwangu.
19 Hivyo, mfalme Agripa, sikuweza kuasi maono ya mbinguni, 20 lakini, kwa wale
walio katika Dameski kwanza, na kisha Yerusalemu na nchi yote ya Yudea, na pia
kwa watu wa mataifa mengine, nilihubiri kwamba watubu na kumgeukia Mungu,
wafanye matendo yanayostahili toba. 21 Kwa sababu hiyo Wayahudi walinikamata
hekaluni, wakajaribu kuniua. 22 Mungu amenisaidia mpaka sasa, hivyo nasimama
na kushuhudia kwa watu wa kawaida na kwa wale wakubwa juu ya yale ambayo
manabii na Musa walisema yatatokea na si vingine; 23 kwamba Kristo lazima
atateseka na atakuwa wa kwanza kufufuka kutoka kwa wafu na kutangaza mwanga
kwa Wayahudi na watu wa mataifa. 24 Paulo alipomaliza kujitetea, Festo alisema kwa
sauti kubwa, 'Paulo, wewe ni mwendawazimu! masomo yako yamekufanya uwe
mwendawazimu. 25 Lakini Paulo akasema, Mimi si mwendawazimu, mheshimiwa
Festo; lakini kwa ujasiri nasema maneno ya ukweli mtupu. 26 Kwa kuwa mfalme
anajua kuhusu mambo haya; na hivyo, ninaongea kwa uhuru kwake, kwa maana
nina hakika kwamba hakuna lolote lililofichwa kwake; kwa kuwa hili halijafanywa
pembeni. 27 Je, unaamini manabii, Mfalme Agripa? Najua kwamba unaamini. '
28 Agripa akamwambia Paulo, 'Kwa muda mfupi unaweza kunishawishi mimi na
kunifanya Mkristo? 29 Paulo akasema, '“Namwomba Mungu kwamba, kwa muda
mfupi au mrefu, si wewe tu, bali pia wote wanaonisikia leo, wawe kama mimi,
lakini bila hii minyororo ya gerezani.” 30 Ndipo mfalme alisimama, na liwali, na
Bernike pia, na wale waliokuwa wamekaa pamoja nao, 31 walipoondoka ukumbini,
walizungumzia wao kwa wao na kusema, 'Mtu huyu hastahili kifo wala kifungo.'
32 Agripa akamwambia Festo, “Mtu huyu angeweza kuwekwa huru kama asingekata
rufani kwa Kaisari.”

# 27

1 Ilipoamuliwa kwamba tunatakiwa tusafiri kwa maji kwenda Italia, walimkabidhi
Paulo na wafungwa wengine kwa afisa mmoja wa jeshi la Kiroma aliyeitwa Julio,
wa Kikosi cha Agustani. 2 Tukapanda meli kutoka Adramitamu, ambayo ilikuwa
isafiri kandokando ya pwani ya Asia. Hivyo tukaingia baharini. Aristaka kutoka
Thesolanike ya Makedonia akaenda pamoja nasi. 3 Siku iliyofuata tukatua nanga
katika mji wa Sidoni, ambapo Julio alimtendea Paulo kwa ukarimu na akamruhusu
kwenda kwa rafiki zake kupokea ukarimu wao. 4 Kutoka hapo tukaenda baharini
tukasafiri kuzunguka kisiwa cha Kipro ambacho kilikuwa kimeukinga upepo, kwa
sababu upepo ulikuwa ukitukabili. 5 Baada ya kuwa tumesafiri katika maji yaliyo
karibu na Kilikia na Pamfilia, tukaja Mira, mji wa Lisia. 6 Pale yule afisa wa jeshi
la Kiroma, akaikuta meli kutoka Alexandria ambayo ilikuwa isafiri kuelekea Italia.
Akatupandisha ndani yake. 7 Baada ya kuwa tumesafiri polepole kwa siku nyingi
na hatimaye tukawa tumefika kwa taabu karibu na Kinidas, upepo haukuturuhusu
tena kuelekea njia hiyo, hivyo tukasafiri kandokando ya kivuli cha Krete tukiukinga
upepo, mkabala na Salmone. 8 Tukasafiri kandokando ya pwani kwa ugumu,
mpaka tukafika mahali palipoitwa Fari Haveni ambayo iko karibu na mji wa Lasi.
9 Tulikuwa tumechukua muda mwingi sana, na muda wa mfungo wa Kiyahudi
ulikuwa umepita pia, na sasa ilikuwa ni hatari kuendelea kusafiri. Hivyo Paulo
akatuonya, 10 na kusema, “Wanaume, naona safari ambayo tunataka tuichukue
itakuwa na madhara na hasara nyingi, siyo tu ya mizigo na meli, lakini pia ya
maisha yetu.” 11 Lakini afisa wa jeshi la Kiroma akamsikiliza zaidi bwana wake
na mmiliki wa meli, kuliko mambo yale ambayo yalizungumzwa na Paulo. 12 Kwa
sababu bandari haikuwa sehemu rahisi kukaa wakati wa baridi, mabaharia wengi
wakashauri tusafiri kutoka pale, ili kwa namna yoyote tukiweza kuufikia mji wa
Foinike, tukae pale wakati wa baridi. Foinike ni bandari huko Krete, na inatazama
kaskazini mashariki na kusini mashariki. 13 Upepo wa kusini ulipoanza kuvuma
polepole, mabaharia wakafikiri wamepata kile ambacho walikuwa wanakihitaji.
Wakang'oa nanga na kusafiri kandokando ya Krete karibu na pwani. 14 Lakini baada
ya muda mfupi upepo mkali, ulioitwa Wa kaskazini mashariki, ukaanza kutupiga
kutoka ng'ambo ya kisiwa. 15 Wakati meli ilipolemewa na kushindwa kuukabili
upepo, tukakubaliana na hali hiyo, tukasafirishwa nao. 16 Tukakimbia kupitia ule
upande uliokuwa unaukinga upepo wa kisiwa kiitwacho Kauda; na kwa taabu sana
tulifanikiwa kuuokoa mtumbwi. 17 Baada ya kuwa wameivuta, walitumia kamba
kuifunga meli. Waliogopa kwamba tungeweza kwenda kwenye eneo la mchanga
mwingi la Syiti, hivyo wakashusha nanga na waliendeshwa kandokando. 18 Tulipigwa
kwa nguvu sana na dhoruba, hivyo siku iliyofuata mabaharia wakaanza kutupa
mizigo kutoka melini. 19 Siku ya tatu, mabaharia wakaanza kuyatoa maji kwa mikono
yao wenyewe. 20 Wakati ambapo jua na nyota hazikutuangazia kwa siku nyingi,
bado dhoruba kubwa ilitupiga, na matumaini kwamba tungeokolewa yalitoweka.
21 Baada ya kuwa wameenda muda mrefu bila chakula, hapo Paulo akasimama
katikati ya mabaharia akasema, “Wanaume, mlipaswa mnisikilize, na tusingengo'a
nanga kutoka Krete, ili kupata haya madhara na hasara. 22 Na sasa nawafariji mjitie
moyo, kwa sababu hakutakuwa upotevu maisha kati yenu, isipokuwa hasara ya
meli tu. 23 Kwa sababu usiku uliopita malaika wa Mungu, ambaye huyo Mungu
mimi ni wake, na ambaye ninamwabudu pia - malaika wake alisimama pembeni
mwangu 24 na kusema, “Usiogope Paulo. Lazima usimame mbele ya Kaisari, na
tazama, Mungu katika wema wake amekupa hawa wote ambao wanasafiri pamoja
nawe. 25 Hivyo, wanaume, jipeni moyo, kwa sababu namwamini Mungu, kwamba
itakuwa kama nilivyoambiwa. 26 Lakini lazima tuumie kwa kupigwa katika baadhi

ya visiwa.” 27 Ulipofika usiku wa kumi na nne, tulipokuwa tukiendeshwa huko na
huko kwenye bahari ya Adratik, kama usiku wa manane hivi, mabaharia walifikiri
kwamba wamekaribia nchi kavu. 28 Walitumia milio kupima kina cha maji na
wakapata mita thelathini na sita, baada ya muda mfupi wakapima tena wakapata
mita ishirini na saba. 29 Waliogopa kwanza tunaweza kugonga miamba, hivyo
wakashusha nanga nne kutoka katika sehemu ya kuwekea nanga na wakaomba
kwamba asubuhi ingekuja mapema. 30 Wale mabaharia walikuwa wanatafuta namna
ya kuitelekeza ile meli na walizishusha majini boti ndogo ndogo za kuokolea maisha,
na wakajifanya kwamba wanatupa nanga kutoka sehemu ya mbele ya boti. 31 Lakini
Paulo akamwambia yule askari wa jeshi la Kiroma na wale askari, “Hamuwezi
kuokoka isipokuwa hawa watu wanabaki kwenye meli”. 32 Kisha wale askari
wakakata kamba za ile boti na ikaachwa ichukuliwe na maji. 33 Wakati mwanga
wa asubuhi ulipokuwa unajitokeza, Paulo akawasihi wote angalau wale kidogo.
Akasema, “Hii ni siku ya kumi na nne mnasuburi bila kula, hamjala kitu. 34 Hivyo
nawasihi mchukue chakula kidogo, kwa sababu hii ni kwa ajili ya kuishi kwenu; na
hakuna hata unywele mmoja wa vichwa vyenu utakaopotea. 35 Alipokwisha kusema
hayo, akachukua mkate akamshukuru Mungu mbele ya macho ya kila mtu. Kisha
akaumega mkate akaanza kula. 36 Kisha wote wakatiwa moyo na wao wakachukua
chakula. 37 Tulikuwa watu 276 ndani ya meli. 38 Walipokwisha kula vya kutosha,
waliifanya meli nyepesi kwa kutupa ngano ndani ya bahari. 39 Ilipokuwa mchana,
hawakuitambua nchi kavu, lakini wakaona sehemu ya nchi kavu iliyoingia majini
iliyokuwa na mchanga mwingi. wakajadiliana kama wanaweza kuiendesha meli
kuelekea hapo. 40 Hivyo wakazilegeza nanga wakaziacha baharini. Katika muda huo
huo wakazilegeza kamba za tanga na wakaiinua sehemu ya mbele kuelekea kwenye
upepo, hivyo wakaelekea kwenye hiyo sehemu ya mchanga mwingi. 41 Lakini wakaja
mahali ambapo mikondo miwili ya maji inakutana, na meli ikaelekea mchangani. Na
ile sehemu ya mbele ya meli ikakwama pale na haikuweza kutoka, lakini sehemu ya
mbele ya meli ikaanza kuvunjika kwa sababu ya ukali wa mawimbi. 42 Mpango wa
wale askari ulikuwa ni kuwaua wafungwa, ili kwamba hakuna ambaye angeogelea
na kutoroka. 43 Lakini yule askari wa jeshi la Kiroma alitaka kumwokoa Paulo, hivyo
akausimamisha mpango wao; na akawaamuru wale ambao wanaweza kuogelea,
waruke kutoka melini kwanza na waende nchi kavu. 44 Kisha wanaume wengine
watafuata, wengine juu ya vipande vya mbao na wengine juu ya vitu vingine kutoka
kwenye meli. Kwa njia hii ikatokea kwamba wote tutafika salama nchi kavu.

# 28

1 Tulipofikishwa salama, tulitambua kwamba kisiwa kinaitwa Malta. 2 Watu
wenyeji wa pale si tu kwamba walitupa ukarimu wa kawaida, bali waliwasha moto
na kutukaribisha sote, kwa sababu ya mvua na baridi iliyokuwa ikiendelea. 3 Lakini
Paulo alipokuwa amekusanya mzigo wa kuni na kuuweka motoni, nyoka mdogo
mwenye sumu akatoka kwenye zile kuni kwa sababu ya lile joto, na akajizungusha
kwenye mkono wake. 4 Watu wenyeji wa pale walipoona mnyama ananing'inia
kutoka kwenye mkono wake, wakasemezana wao kwa wao, “Mtu huyu hakika ni
muuaji ambaye ametoroka baharini, lakini haki haimuruhusu kuishi.” 5 Lakini
yeye akamtupia huyo mnyama katika moto na hakupata madhara yoyote. 6 Wao
walimngojea avimbe kwa homa au aanguke ghafla na kufa. Lakini baada ya
kumwangalia kwa muda mrefu na kuona kwamba hakuna jambo ambalo si la
kawaida kwake, walibadilisha mawazo yao na kusema alikuwa mungu. 7 Basi
mahali pale karibu palikuwa na ardhi ambayo ilikuwa mali ya mkuu wa kisiwa, mtu
aliyeitwa Pablio. Alitukaribisha na kutukarimu kwa siku tatu. 8 Ilitokea kwamba

baba wa Pablio alishikwa na homa na ugonjwa wa kuhara. Na Paulo alipomwendea,
aliomba, akaweka mikono juu yake, na kumponya. 9 Baada ya hili kutokea, watu
wengine pale kisiwani waliokuwa wanaumwa pia walikwenda na waliponywa.
10 Watu wakatuheshimu kwa heshima nyingi. Tulipokuwa tunajiandaa kusafiri,
walitupa vile tulivyovihitaji. 11 Baada ya miezi mitatu, tulisafiri ndani ya meli ya
Iskanda ambayo ilikuwa imepigwa baridi hapo kisiwani, ambayo viongozi wake
walikuwa ndugu wawili mapacha. 12 Baada ya kuwa tumetua katika mji wa Sirakusa,
tulikaa pale siku tatu. 13 Kutokea pale tulisafiri tukafika katika mji wa Regio. Baada
ya siku moja upepo wa kusini ulitokea ghafla, na baada ya siku mbili tukafika katika
mji wa Putoli. 14 Huko tuliwakuta baadhi ya ndugu na tulikaribishwa kukaa nao kwa
siku saba. Kwa njia hii tukaja Rumi. 15 Kutoka huko wale ndugu, baada ya kuwa
wamesikia habari zetu, walikuja kutupokea huko soko la Apias na Hotel tatu. Paulo
alipowaona wale ndugu alimshukuru Mungu akajitia ujasiri. 16 Tulipoingia Roma,
Paulo aliruhusiwa kuishi peke yake pamoja na yule askari aliyekuwa akimlinda.
17 Basi ilikuwa baada ya siku tatu Paulo aliwaita pamoja wale wanume waliokuwa
viongozi kati ya Wayahudi. Walipokuja pamoja, alisema kwao, “Ndugu, pamoja na
kwamba sijafanya kosa lolote kwa watu hawa au kufanya kinyume na taratibu za
mababa zetu waliotutangulia, nilitolewa kama mfungwa kutoka Yerusalemu hadi
kwenye mikono ya Warumi. 18 Baada ya kunihoji, walitamani kuniacha huru, kwa
sababu kulikuwa hakuna sababu kwangu mimi ya kustahili adhabu ya kifo. 19 Lakini
wale Wayahudi walipoongea kinyume cha shauku yao, nililazimika kukata rufaa kwa
Kaisaria, japokuwa haikuwa kana kwamba naleta mashtaka juu ya taifa langu. 20 Kwa
sababu ya kukata kwangu rufaa, hivyo, niliomba kuwaona na kuongea nanyi. Ni
kwa sababu ya kile ambacho Israel anaujasiri kwacho, nimefungwa na kifungo hiki.
21 Kisha wakamwambia, “Hatujawahi kupokea barua kutoka Yudea kukuhusu wewe,
wala hakuna ndugu aliyekuja na kutoa taarifa au kusema neno lolote baya kuhusu
wewe. 22 Lakini tunataka kusikia kutoka kwako unafikiri nini kuhusu hili kundi la
watu hawa, kwa sababu inajulikana kwetu kwamba linaongea kinyume kila mahali.”
23 Walipokuwa wametenga siku kwa ajili yake, watu wengi zaidi walimwijia mahali
alipokuwa anaishi. Alisema lile jambo kwao na kushuhudia kuhusu ufalme wa
Mungu. Alijaribu kuwashawishi kuhusu Yesu, kwa namna zote mbili kutoka katika
sheria za Musa na kutoka kwa manabii, kuanzia asubuhi hadi jioni. 24 Baadhi yao
walishawishika kuhusu mambo yale yaliyosemwa, wakati wengine hawakuamini.
25 Waliposhindwa kukubaliana wao kwa wao, waliondoka baada ya Paulo kulisema
jambo hili moja, “Roho Mtakatifu alisema vyema kupitia Isaya nabii kwa baba
zenu. 26 Alisema, 'Nenda kwa watu hawa useme, “Kwa masikio yenu mtasikia,
lakini hamtaelewa; Na kwa macho yenu mtaona lakini hamtatambua. 27 Kwa
ajili ya mioyo ya watu hawa imekuwa dhaifu, masikio yao yamesikia kwa taabu,
wamefumba macho yao; ili kwamba wasijekutambua kwa macho yao, na kusikia
kwa masikio yao, na kuelewa kwa mioyo yao, na kugeuka tena, na ningeliwaponya.”'
28 Kwa hiyo, mnapaswa kujua kwamba huu wokovu wa Mungu umepelekwa kwa
watu wa Mataifa, na watasikiliza.” (Zingatia: Mstari huu 29 “Wakati alipokuwa
amesema mambo haya, wayahudi waliondoka, wakiwa na mashindano makubwa
kati yao.,” haumo kwenye nakala bora za kale). 30 Paulo alikaa katika nyumba yake ya
kupanga kwa miaka yote miwili, na aliwakaribisha wote waliokuja kwake. 31 Alikuwa
akihubiri ufalme wa Mungu na alikuwa akifundisha mambo juu ya Bwana Yesu Kristo
kwa ujasiri wote. Hakuna aliyemzuia.

# Warumi

1 Paulo, mtumishi wa Yesu Kristo, aliyeitwa kuwa mtume, na kutengwa kwa ajili
ya Injili ya Mungu. 2 Hii ndio ile Injili aliyoiahidi zamani kupitia manabii wake
katika maandiko matakatifu. 3 Ni kuhusu Mwana wake, aliyezaliwa kutoka ukoo
wa Daudi kwa jinsi ya mwili. 4 Yeye alitangazwa kwa Mwana wa Mungu kwa nguvu
ya Roho ya utakatifu kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu. 5 Kupitia yeye
tumepokea neema na utume kwa utii wa imani kati ya mataifa yote, kwa ajili ya jina
lake. 6 Kati ya mataifa haya, ninyi pia mmeitwa kuwa wa Yesu Kristo. 7 Barua hii ni
kwa wote walioko Rumi, wapendwao na Mungu, walioitwa kuwa watu watakatifu.
Neema na iwe kwenu, na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu
Kristo. 8 Kwanza, namshukuru Mungu wangu katika Yesu Kristo kwa ajili yenu nyote,
kwa sababu imani yenu inahubiriwa katika dunia nzima. 9 Kwa maana Mungu
ni shahidi wangu, ambaye ninamtumikia kwa roho yangu katika injili ya Mwana
wake, jinsi ninavyodumu katika kuwataja. 10 Daima naomba katika sala zangu
kwamba kwa njia yoyote nipate mwishowe kuwa na mafanikio sasa kwa mapenzi
ya Mungu katika kuja kwenu. 11 Maana natamani kuwaona, ili nipate kuwapa ninyi
baadhi ya karama za rohoni, nipate kuwaimarisha. 12 Yaani, natazamia kutiwa moyo
pamoja nanyi, kwa njia ya imani ya kila mmoja wetu, yenu na yangu. 13 Sasa
ndugu, sitaki mkose kufahamu kwamba, mara nyingi nimekusudia kuja kwenu, lakini
nimezuiliwa mpaka sasa. Nilitaka hivi ili kuwa na matunda kwenu kama ilivyo pia
miongoni mwa watu wa mataifa. 14 Nadaiwa na Wayunani na wageni pia, werevu
na wajinga. 15 Kwa hiyo, kwa upande wangu, mimi niko tayari kutangaza injili
kwenu pia ninyi mlio huko Roma. 16 Kwa maana siionei haya injili, kwa kuwa
ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na
kwa Myunani pia. 17 Kwa maana haki ya Mungu imedhihirishwa kutoka imani hata
imani, kama ilivyo andikwa, “Mwenye haki ataishi kwa imani.” 18 Maana ghadhabu
ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni dhidi ya uasi na uovu wote wa watu,
ambao kwa njia ya udhalimu huificha kweli. 19 Hii ni kwa sababu, yote yanayoweza
kujulikana juu ya Mungu ni wazi kwao. Maana Mungu amewafahamisha. 20 Maana
mambo yake yasioonekana vizuri yamekuwa wazi tangu kuumbwa kwa ulimwengu.
Yanaeleweka kupitia vitu vilivyoumbwa. Mambo haya ni uwezo wake wa milele
na asili ya uungu. Matokeo yake, watu hawa hawana udhuru. 21 Hii ni kwa
sababu, ingawa walijua kuhusu Mungu, hawakumtukuza yeye kama Mungu, wala
hawakumpa shukrani. Badala yake, wamekuwa wapumbavu katika mawazo yao,
na mioyo yao yenye ujinga ilitiwa giza. 22 Walijiita kuwa ni werevu, lakini wakawa
wajinga. 23 Waliubadili utukufu wa Mungu asie na uharibifu kwa mfano wa sura
ya binadamu aliye na uharibifu, na ya ndege, ya wanyama wenye miguu minne, na
ya viumbe vitambaavyo. 24 Kwa hiyo Mungu aliwaacha wafuate tamaa za mioyo
yao kwa uchafu, kwa miili yao kufedheheshwa baina yao. 25 Ni wao walioibadili
kweli ya Mungu kuwa uongo, na ambao waliabudu na kutumikia viumbe badala ya
Muumbaji, ambaye anasifiwa milele. Amina. 26 Kwa sababu hii, Mungu aliwaacha
wafuate tamaa zao za aibu, kwa kuwa wanawake wao walibadilisha matumizi yao
ya asili kwa kile kilicho kinyume na asili. 27 Hali kadhalika, wanaume pia wakaacha
matumizi yao ya asili kwa wanawake na kuwakwa na tamaa dhidi yao wenyewe.
Hawa walikuwa wanaume ambao walifanya na wanaume wenzao yasiyo wapasa, na
ambao walipokea adhabu iliyostahili upotovu wao. 28 Kwa sababu walikataa kuwa
na Mungu katika fahamu zao, aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa, wafanye mambo

yale yasiyofaa. 29 Wamejawa na udhalimu wote, uovu, tamaa na ubaya. Wamejawa
na wivu, uuaji, ugomvi, udanganyifu, na nia mbaya. 30 Wao pia ni wasengenyaji,
wasingiziaji, na wenye kumchukia Mungu. Wenye vurugu, kiburi, na majivuno. Wao
ni watunga mabaya, na wasiotii wazazi wao. 31 Wao hawana ufahamu; wasioaminika,
hawana mapenzi ya asili, na wasio na huruma. 32 Wanaelewa kanuni za Mungu,
ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo wanastahili kifo. Lakini si tu
wanafanya mambo hayo, wao pia wanakubaliana na wale wanaofanya mambo hayo.

# 2

1 Kwa hiyo hauna udhuru, wewe uhukumuye, kwa maana katika yale uhukumuyo
mwingine wajitia hatiani mwenyewe. Kwa maana wewe uhukumuye unafanya
mambo yale yale. 2 Lakini twajua kwamba hukumu ya Mungu ni ya kweli juu
yao wafanyao mambo kama hayo. 3 Lakini wewe tafakari hili, wewe ambaye
unahukumu wale wanaotenda mambo hayo ingawa nawe unafanya mambo yayo
hayo. Je utaepuka hukumu ya Mungu? 4 Au unafikiri kidogo sana juu ya wingi wa
wema wake, kuchelewa kwa adhabu yake, na uvumilivu wake? Je, hujui kwamba
wema wake unapaswa kukuelekeza katika toba? 5 Bali kwa kadiri ya ugumu wako
na kwa moyo wako usio na toba wajiwekea mwenyewe akiba ya ghadhabu kwa
siku ile ya ghadhabu, yaani, siku ile ya ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu.
6 Yeye atamlipa kila mtu kipimo sawa na matendo yake: 7 kwa wale ambao kwa
uthabiti wa matendo mema wametafuta sifa, heshima na kutokuharibika, atawapa
uzima wa milele. 8 Lakini kwa wale ambao ni wabinafsi, wasioitii kweli bali hutii
dhuluma, ghadhabu na hasira kali itakuja. 9 Mungu ataleta dhiki na shida juu ya
kila nafsi ya binadamu aliyefanya uovu, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani
pia. 10 Lakini sifa, heshima na amani itakuja kwa kila mtu atendaye mema, kwa
Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia. 11 Kwa maana hakuna upendeleo kwa
Mungu. 12 Kwa maana kama vile wengi waliokosa pasipo sheria watapotea pasipo
sheria, na kama vile wengi waliokosa kulingana na sheria watahukumiwa kwa
sheria. 13 Maana si wasikiaji wa sheria walio wenye haki mbele za Mungu, bali
ni wale waitendao sheria watakaohesabiwa haki. 14 Kwa maana watu wa Mataifa,
ambao hawana sheria, wanafanya kwa asili mambo ya sheria, wao, wamekuwa
sheria kwa nafsi zao, ingawa wao hawana sheria. 15 Kwa hili wanaonesha kwamba
matendo yanayohitajika kwa mujibu wa sheria yameandikwa ndani ya mioyo yao.
Dhamiri zao pia zinawashuhudia wao, na mawazo yao wenyewe ama huwashitaki
au huwalinda wao wenyewe 16 na pia kwa Mungu. Haya yatatokea katika siku
ambayo Mungu atazihukumu siri za watu wote, sawasawa na injili yangu, kwa njia
ya Yesu Kristo. 17 Tuseme kwamba unajiita mwenyewe Myahudi, aliyekaa katika
sheria, shangilia kwa kujisifu katika Mungu, 18 yajue mapenzi yake, na kupima
mambo ambayo yanatofautiana nayo, baada ya kuagizwa na sheria. 19 Na tuseme
kwamba una ujasiri kwamba wewe mwenyewe ni kiongozi wa kipofu, mwanga kwa
wale walio gizani, 20 msahihishaji wa wajinga, mwalimu wa watoto, na kwamba
unayo katika sheria jinsi ya elimu na kweli. 21 Wewe basi, uhubiriye mwingine,
je, hujifundishi mwenyewe? Wewe uhubiriye kutokuiba, je wewe huiba? 22 Wewe
usemae usizini, je unazini? Wewe uchukiaye sanamu, je unaiba hekaluni? 23 Wewe
ujisifuye katika sheria, je haumfedheheshi Mungu katika kuvunja sheria? 24 Kwa
maana “jina la Mungu linafedheheshwa kati ya watu wa mataifa kwa sababu
yenu,” kama ilivyoandikwa. 25 Kwa maana Kutahiriwa kweli kwafaa kama ukitii
sheria, lakini kama wewe ni mkiukaji wa sheria, kutahiriwa kwako kunakuwa
kutokutahiriwa. 26 Basi, ikiwa, mtu asiyetahiriwa anaendelea kushika matakwa ya
sheria, je kutokutahiriwa kwake hakutachukuliwa kana kwamba ametahiriwa? 27 Na

yeye asiyetahiriwa kwa asili hatakuhukumu kama akitimiza sheria? Hii ni kwa
sababu una maandiko yaliyoandikwa na tohara pia lakini bado u mkiukaji wa sheria!
28 Kwa maana yeye si Myahudi aliye kwa hali ya nje; wala kutahiriwa si kule ambako
ni kwa nje tu katika mwili. 29 Lakini yeye ni Myahudi aliye kwa ndani, na tohara ni
ya moyo, katika roho, si katika andiko. Sifa ya mtu wa namna hiyo haitokani na watu
bali yatoka kwa Mungu.

# 3

1 Kisha ni faida gani aliyo nayo Myahudi? Na faida ya tohara ni nini? 2 Ni
vyema sana kwa kila njia. Awali ya yote, Wayahudi walikabidhiwa ufunuo kutoka
kwa Mungu. 3 Lakini, itakuwaje iwapo baadhi ya Wayahudi hawakuwa na imani?
Je, kutokuamini kwao kutafanya uaminifu wa Mungu kuwa batili? 4 La hasha.
Badala yake, acha Mungu aonekane kuwa kweli, hata kama kila mtu ni mwongo.
Kama ilivyokuwa imeandikwa, “Ya kwamba uweze kuonekana kuwa mwenye haki
katika maneno yako, na uweze kushinda uingiapo katika hukumu.” 5 Lakini ikiwa
uovu wetu unaonesha haki ya Mungu, tuseme nini? Mungu si dhalimu atoapo
ghadhabu yake, je yupo hivyo? Naongea kutokana na mantiki ya kibinadamu. 6 La
hasha! Ni jinsi gani basi Mungu atauhukumu ulimwengu? 7 Lakini ikiwa kweli ya
Mungu kupitia uongo wangu hutoa sifa tele kwa ajili yake, kwa nini ningali bado
nahukumiwa kama mwenye dhambi? 8 Kwa nini tusiseme, kama tulivyosingiziwa
na kama wengine wanavyothibitisha kwamba tunasema, “Tufanye uovu, ili mema
yaje”? Hukumu juu yao ni ya haki. 9 Ni nini basi? Tunajitetea wenyewe? Hapana
kabisa. Kwa kuwa sisi tayari tumewatuhumu Wayahudi na Wayunani wote pamoja,
ya kuwa wapo chini ya dhambi. 10 Hii ni kama ilivyoandikwa: “Hakuna mwenye haki,
hata mmoja. 11 Hakuna mtu ambaye anaelewa. Hakuna mtu ambaye anamtafuta
Mungu. 12 Wote wamegeuka. Wao kwa pamoja wamekuwa hawana maana. Hakuna
atendaye mema, la, hata mmoja. 13 Makoo yao ni kaburi lililo wazi. Ndimi zao
zimedanganya. Sumu ya nyoka ipo chini ya midomo yao. 14 Vinywa vyao vimejaa
laana na uchungu. 15 Miguu yao ina mbio kumwaga damu. 16 Uharibifu na mateso
yapo katika njia zao. 17 Watu hawa hawajajua njia ya amani. 18 Hakuna hofu ya
Mungu mbele ya macho yao.” 19 Sasa tunajua kwamba chochote sheria isemacho,
husema na wale walio chini ya sheria. Hii ni ili kwamba kila kinywa kifungwe,
na hivyo kwamba ulimwengu wote uweze kuwajibika kwa Mungu. 20 Hii ni kwa
sababu hakuna mwili utakaohesabiwa haki kwa matendo ya sheria mbele za macho
yake. Kwa kuwa kupitia Sheria huja ufahamu wa dhambi. 21 Lakini sasa pasipo
sheria, haki ya Mungu imejulikana. Ilishuhudiwa kwa sheria na Manabii, 22 hiyo
ni, haki ya Mungu kupitia imani katika Yesu Kristo kwa wale wote wanaoamini.
Maana hakuna tofauti. 23 Kwa kuwa wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa
na utukufu wa Mungu. 24 Wamehesabiwa haki bure kwa neema yake kwa njia ya
ukombozi ulio katika Kristo Yesu. 25 Kwa maana Mungu alimtoa Kristo Yesu awe
upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake. Alimtoa Kristo kama ushahidi wa
haki yake, kwa sababu ya kuziachilia dhambi zilizopita 26 katika uvumilivu wake.
Haya yote yalitokea ili kuonesha haki yake wakati huu wa sasa. Hii ilikuwa ili aweze
kujithibitisha mwenyewe kuwa haki, na kuonesha kwamba humhesabia haki mtu
yeyote kwa sababu ya imani katika Yesu. 27 Kuwapi basi kujisifu? Kumetengwa. Kwa
misingi ipi? Misingi ya matendo? Hapana, lakini kwa misingi ya imani. 28 Hivyo
tunahitimisha kwamba mtu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria.
29 Au Mungu ni Mungu wa Wayahudi tu? Je yeye si Mungu wa watu wa Mataifa pia?
Ndiyo, wa mataifa pia. 30 Ikiwa kwa kweli Mungu ni mmoja, atawahesabia haki walio

wa tohara kwa imani, na wasiotahiriwa kwa njia ya imani. 31 Je sisi twaibatilisha
sheria kwa imani? La hasha! Kinyume cha hayo, sisi twaithibitisha sheria.

# 4

1 Tutasema nini tena kwamba Abrahamu, baba yetu kwa jinsi ya mwili,
amepatikana? 2 Kwa maana ikiwa Abrahamu alihesabiwa haki kwa matendo,
angekuwa na sababu ya kujisifu, lakini si mbele za Mungu. 3 Kwani maandiko
yanasemaje? "Abrahamu alimwamini Mungu, na ikahesabiwa kwake kuwa haki."
4 Sasa kwa mtu afanyaye kazi, malipo yake hayahesabiwi kuwa ni neema, bali kuwa
ni deni. 5 Lakini kwa mtu asiyefanya kazi bali anamwamini yeye ambaye amhesabia
haki asiyekuwa mtaua, imani yake mtu huyo imehesabiwa kuwa haki. 6 Daudi
pia hunena baraka juu ya mtu ambaye Mungu amhesabia haki pasipo matendo.
7 Alisema, "Wamebarikiwa wale ambao maovu yao yamesamehewa na ambao
dhambi zao zimefunikwa. 8 Amebarikiwa mtu yule ambaye Bwana hamhesabii
dhambi." 9 Basi je baraka hizi ni kwa wale waliotahiriwa tu, au pia kwa wale
wasiotahiriwa? Kwa maana twasema, "kwa Abrahamu imani yake ilihesabiwa
kuwa ni haki." 10 Hivyo ilihesabiwaje basi? Wakati Abrahamu alikuwa katika
tohara, au kabla hajatahiriwa? Haikuwa katika kutahiriwa, bali katika kutotahiriwa.
11 Abrahamu alipokea alama ya kutahiriwa. Huu ulikuwa muhuri wa ile haki ya
imani aliyokuwa nayo tayari kabla hajatahiriwa. Matokeo ya ishara hii ni kwamba
alifanyika kuwa baba wa wote waaminio, hata kama wapo katika kutotahiriwa. Hii
ina maana kwamba haki itahesabiwa kwao. 12 Hii pia ilimaanisha kuwa Abrahamu
alifanyika baba wa tohara si tu kwa wale wanaotokana na tohara, bali pia wale
wanaozifuata nyayo za baba yetu Abrahamu. Na hii ndiyo imani aliyokuwa nayo
kwa wasiotahiriwa. 13 Kwa maana haikuwa kwa sheria kwamba ahadi ilitolewa
kwa Abrahamu na uzao wake, ahadi hii ya kwamba watakuwa warithi wa dunia.
isipokuwa, ilikuwa kupitia haki ya imani. 14 Kwa maana kama wale wa sheria ndio
warithi, imani imekuwa bure, na ahadi imebatilika. 15 Kwa sababu sheria huleta
ghadhabu, lakini pale ambapo hakuna sheria, pia hakuna kutotii. 16 Kwa sababu hii
hili hutokea kwa imani, ili iwe kwa neema. Matokeo yake, ahadi ni dhahiri kwa
uzao wote. Na wazawa hawa si tu wale wanaojua sheria, bali pia wale ambao ni wa
imani ya Abrahamu. Kwa maana yeye ni baba yetu sisi sote, 17 kama ilivyoandikwa,
"Nimekufanya wewe kuwa baba wa mataifa mengi." Abrahamu alikuwa katika
uwepo wa yule aliyemwamini, yaani, Mungu ambaye huwapa wafu uzima na kuyaita
mambo ambayo hayapo ili yaweze kuwepo. 18 Licha ya hali zote za nje, Abrahamu
kwa ujasiri alimuamini Mungu kwa siku zijazo. Hivyo akawa baba wa mataifa
mengi, kulingana na kile kilichonenwa,"... Ndivyo utakavyokuwa uzao wako." 19 Yeye
hakuwa dhaifu katika imani. Abrahamu alikiri kwamba mwili wake mwenyewe
ulikwisha kufa - alikuwa na umri wa karibu miaka mia moja. Pia alikubaliana na
hali ya kufa ya tumbo la Sara. 20 Lakini kwa sababu ya ahadi ya Mungu, Abrahamu
hakusita katika kutokuamini. Bali, alitiwa nguvu katika imani na alimsifu Mungu.
21 Alikuwa akijua hakika ya kuwa kile ambacho Mungu ameahidi, alikuwa pia na
uwezo wa kukikamilisha. 22 Kwa hiyo hii pia ilihesabiwa kwake kuwa ni haki.
23 Sasa haikuandikwa tu kwa faida yake, kwamba ilihesabiwa kwake. 24 Iliandikwa
kwa ajili yetu pia, kwa waliowekewa kuhesabiwa, sisi ambao tunaamini katika yeye
aliyemfufua Bwana wetu Yesu kutoka wafu. 25 Huyu ni yule ambaye alitolewa kwa
ajili ya makosa yetu na kufufuliwa ili tupate kuhesabiwa haki.

# 5

1 Kwa kuwa tumehesabiwa haki kwa njia ya imani, tuna amani na Mungu kwa

njia ya Bwana wetu Yesu Kristo. 2 Kupitia yeye sisi pia tuna fursa kwa njia ya imani
katika neema hii ambayo ndani yake tunasimama. Tunafurahi katika ujasiri atupao
Mungu kwa ajili ya baadaye, ujasiri ambao tutashiriki katika utukufu wa Mungu.
3 Siyo hili tu, lakini pia tunafurahi katika mateso yetu. Tunajua kwamba mateso
huzaa uvumilivu. 4 Uvumilivu huzaa kukubalika, na kukubalika huzaa ujasiri kwa
ajili ya baadaye. 5 Ujasiri huu haukatishi tamaa, kwa sababu upendo wa Mungu
umemwagwa katika mioyo yetu kupitia Roho Mtakatifu, ambaye alitolewa kwetu.
6 Kwa tulipokuwa tungali tu dhaifu, kwa wakati muafaka Kristo alikufa kwa ajili ya
waovu. 7 Kwa kuwa itakuwa vigumu mmoja kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki. Hii
ni kwamba, pengine mtu angethubutu kufa kwa ajili ya mtu mwema. 8 Lakini Mungu
amehakikisha upendo wake mwenyewe kwetu, kwa sababu wakati tulipokuwa
tungali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yetu. 9 Kisha zaidi ya yote, sasa
kwa kuwa tumehesabiwa haki kwa damu yake, tutaokolewa kwa hiyo kutoka katika
gadhabu ya Mungu. 10 Kwa kuwa, ikiwa wakati tulipokuwa maadui, tulipatanishwa
na Mungu kwa njia ya kifo cha mwanae, zaidi sana, baada ya kuwa tumekwisha
patanishwa, tutaokolewa kwa maisha yake. 11 Siyo hivi tu, bali pia tunafurahi katika
Mungu kupitia Bwana Yesu Kristo, kupitia yeye ambaye sasa tumepokea upatanisho
huu. 12 Kwa hiyo basi, kama kupitia mtu mmoja dhambi iliingia duniani, kwa njia hii
kifo kiliingia kwa njia ya dhambi. Na kifo kikasambaa kwa watu wote, kwa sababu
wote walifanya dhambi. 13 Kwa kuwa hadi sheria, dhambi ilikuwa duniani, lakini
dhambi haihesabiki wakati hakuna sheria. 14 Hata hivyo, kifo kilitawala kutoka
Adamu hadi Musa, hata juu ya wale ambao hawakufanya dhambi kama kutotii kwa
Adamu, ambaye ni mfano wa yeye ambaye angekuja. 15 Lakini hata hivyo, zawadi
ya bure si kama kosa. Kwa kuwa ikiwa kwa kosa la mmoja wengi walikufa, zaidi
sana neema ya Mungu na zawadi kwa neema ya mtu mmoja, Yesu Kristo, imezidi
kuongezeka kwa wengi. 16 Kwa kuwa zawadi si kama matokeo ya yule ambaye
alifanya dhambi. Kwa kuwa kwa upande mwingine, hukumu ya adhabu ilikuja
kwa sababu ya kosa la mtu mmoja. Lakini kwa upande mwingine, kipawa cha bure
kinachotoka katika kuhesabiwa haki kilikuja baada ya makosa mengi. 17 Kwa maana,
ikiwa kwa kosa la mmoja, kifo kilitawala kupitia mmoja, zaidi sana wale ambao
watapokea neema nyingi pamoja na kipawa cha haki watatawala kupitia maisha
ya mmoja, Yesu Kristo. 18 Hivyo basi, kama kupitia kosa moja watu wote walikuja
kwenye hukumu, ingawa kupitia tendo moja la haki kulikuja kuhesabiwa haki ya
maisha kwa watu wote. 19 Kwa kuwa kama kupitia kutotii kwa mtu mmoja wengi
walifanywa wenye dhambi, hivyo kupitia utii wa mmoja wengi watafanywa wenye
haki. 20 Lakini sheria iliingia pamoja, ili kwamba kosa liweze kuenea. Lakini mahali
ambapo dhambi ilizidi kuwa nyingi, neema iliongezeka hata zaidi. 21 Hii ilitokea
ili kwamba, kama dhambi ilivyotawala katika kifo, ndivyo hata neema inaweza
kutawala kupitia haki kwa ajili ya maisha ya milele kupitia Yesu Kristo Bwana wetu.

# 6

1 Tuseme nini basi? Tuendelee katika dhambi ili neema iongezeke? 2 La hasha.
Sisi tuliokufa katika dhambi, tunawezaje tena kuishi katika hiyo? 3 Je hamjui ya
kuwa wale waliobatizwa katika Kristo walibatizwa katika mauti yake? 4 Tulikuwa
tumezikwa pamoja naye kupitia ubatizo katika kifo. Hii ilifanyika ili kwamba kama
vile Kristo alivyoinuliwa kutoka mauti kupitia utukufu wa Baba, ili kwamba nasi
tuweze kutembea katika upya wa maisha. 5 Maana ikiwa tumeunganishwa pamoja
naye katika mfano wa kifo chake, pia tutaunganishwa katika ufufuo wake. 6 Sisi
tunajua hivi, utu wetu wa zamani ulisulubiwa pamoja naye, ili kwamba mwili wa
dhambi uharibiwe. Hii ilitokea ili kwamba tusiendelee kuwa watumwa wa dhambi.

[7] Yeye aliyekufa amefanywa mwenye haki kulingana na dhambi. [8] Lakini kama
tumekufa pamoja na Kristo, tunaamini kwamba tutaishi pamoja naye pia. [9] Tunajua
kwamba Kristo amefufuliwa kutoka katika wafu, na kwamba si mfu tena. Kifo
hakimtawali tena. [10] Maana kwa habari ya kifo alichokufa kwa dhambi, alikufa mara
moja kwa ajili ya wote. Hata hivyo, maisha anayoishi, anaishi kwa ajili ya Mungu.
[11] Kwa njia iyo hiyo, nanyi pia mnapaswa kujihesabu kuwa wafu katika dhambi, bali
hai kwa Mungu katika Kristo Yesu. [12] Kwa sababu hiyo usiruhusu dhambi itawale
mwili wako ili kusudi uweze kuzitii tamaa zake. [13] Usitoe sehemu za mwili wako
katika dhambi kama vyombo visivyo na haki, bali jitoeni wenyewe kwa Mungu, kama
walio hai kutoka mautini. Na zitoeni sehemu za miili yenu kama vyombo vya haki
kwa Mungu. [14] Msiiruhusu dhambi iwatawale. Kwa kuwa hamko chini ya sheria, bali
chini ya neema. [15] Nini basi? Tutende dhambi kwa kuwa hatupo chini ya sheria, bali
chini ya neema? La hasha. [16] Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa wenyewe
kama watumishi ndiye ambaye ninyi mnakuwa watumishi wake, yeye mnayepaswa
kumtii? Hii ni kweli hata kama ninyi ni watumwa katika dhambi ambayo inapelekea
mauti, au watumwa wa utii unaopelekea haki. [17] Lakini ashukuriwe Mungu! Kwa
kuwa mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mmetii kutoka moyoni ile namna ya
fundisho mliopewa. [18] Mmefanywa huru kutoka kwenye dhambi, na mmefanywa
watumwa wa haki. [19] Ninazungumza kama mtu kwa sababu ya madhaifu ya miili
yenu. Kwa maana kama vile mlivyotoa viungo vya miili yenu kuwa watumwa kwa
uchafu na uovu, kwa jinsi iyo hiyo, sasa toeni viungo vya miili yenu kuwa watumwa
wa haki kwa utakaso. [20] Kwa kuwa mlipokuwa watumwa wa dhambi, mlikuwa huru
mbali na haki. [21] Kwa wakati huo, mlikuwa na tunda lipi kwa mambo ambayo kwa
sasa mnaona aibu kwayo? Kwa kuwa matokeo ya mambo hayo ni kifo. [22] Lakini
kwa kuwa sasa mmefanywa huru mbali na dhambi na mmefanyika watumwa kwa
Mungu, mna tunda kwa ajili ya utakaso. Tokeo ni uzima wa milele. [23] Kwa kuwa
mshahara wa dhambi ni mauti, bali zawadi ya bure ya Mungu ni uzima wa milele
katika Kristo Yesu Bwana wetu.

# 7

[1] Au hamjui, ndugu zangu (kwa kuwa naongea na watu wanaoijua sheria), kwamba
sheria humtawala mtu anapokuwa hai? [2] Kwa maana mwanamke aliyeolewa
amefungwa na sheria kwa yule mme wake anapokuwa hai, lakini ikiwa mme wake
atakufa, atakuwa amewekwa huru kutoka sheria ya ndoa. [3] Hivyo basi, wakati mme
wake angali akiishi, ikiwa anaishi na mwanamme mwingine, ataitwa mzinzi. Lakini
ikiwa mme wake akifa, yuko huru dhidi ya sheria, hivyo hatakuwa mzinzi ikiwa
anaishi na mwanamme mwingine. [4] Kwa hiyo, ndugu zangu, ninyi pia mlifanywa
wafu kwa sheria kwa njia ya mwili wa Kristo. Imekuwa hivi ili mpate kuunganishwa
na mwingine, kwake yeye ambaye alifufuliwa kutoka wafu ili tuweze kumzalia
Mungu matunda. [5] Kwa maana tulipokuwa katika hali ya mwili, tamaa za dhambi
ziliamshwa katika viungo vyetu kwa njia ya sheria na kuizalia mauti matunda.
[6] Lakini sasa tumefunguliwa kutoka katika sheria. Tumeifia ile hali iliyotupinga. Ili
sisi tupate kutumika katika hali mpya ya Roho, na si katika hali ya zamani ya andiko.
[7] Tusemeje basi? Sheria ni dhambi? La hasha. Hata hivyo, nisingelitambua dhambi,
isingelikuwa kwa njia ya sheria. Kwa kuwa nisingelijua kutamani kama sheria
isingelisema, “Usitamani.” [8] Lakini dhambi ilipata nafasi kwa ile amri na ikaleta
ndani yangu kila aina ya kutamani. Kwa maana dhambi pasipo sheria imekufa.
[9] Nami nilikuwa hai hapo kwanza bila sheria, lakini ilipokuja ile amri, dhambi
ilipata uhai, nami nikafa. [10] Ile amri na ambayo ingelileta uzima iligeuka kuwa
mauti kwangu. [11] Kwa maana dhambi ilipata nafasi kwa ile amri na ikanidanganya.

Kupitia ile amri, iliniua. 12 Hivyo sheria ni takatifu, na ile amri ni takatifu, ya yaki,
na njema. 13 Hivyo basi ile iliyo njema ilikuwa mauti kwangu mimi? Isiwe hivyo
kamwe. Lakini dhambi, ili ionekane kuwa ni dhambi hasa kupitia ile njema, ilileta
mauti ndani yangu. Hii ilikuwa ili kwamba kupitia ile amri, dhambi izidi kuwa mbaya
mno. 14 Kwa maana twajua ya kuwa sheria asili yake ni ya rohoni, lakini mimi
ni mtu wa mwilini. Nimeuzwa chini ya utumwa wa dhambi. 15 Maana nifanyalo,
silielewi dhahiri. Kwa kuwa lile nilipendalo kutenda, silitendi, na lile nilichukialo,
ndilo ninalolitenda. 16 Lakini kama nikilitenda lile nisilolipenda, nakubaliana na
sheria ya kuwa sheria ni njema. 17 Lakini sasa si mimi nafsi yangu ninayetenda hilo,
bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu. 18 Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu,
yaani ndani ya mwili wangu, halikai jambo jema. Kwa kuwa tamaa ya lililo jema
imo ndani yangu, lakini silitendi. 19 Kwa maana lile jema nilipendalo silitendi, bali
lile ovu nisilolipenda ndilo nilitendalo. 20 Sasa kama natenda lile nisilolipenda, si
mimi binafsi nilitendaye, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu. 21 Nimefahama,
tena, imo kanuni ndani yangu ya kutaka kutenda lililo jema, lakini uovu hakika
umo ndani yangu. 22 Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani.
23 Lakini naona kanuni iliyo tofauti katika viungo vya mwili wangu. Inapiga vita
dhidi ya kanuni mpya katika akili zangu. Inanifanya mimi mateka kwa kanuni ya
dhambi iliyo katika viungo vya mwili wangu. 24 Mimi ni mtu wa huzuni! Ni nani
atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? 25 Lakini shukrani kwa Mungu kwa Yesu
Kristo Bwana wetu! Hivyo basi. Mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria
ya Mungu. Bali, kwa mwili naitumikia kanuni ya dhambi.

# 8

1 Kwa hiyo basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu.
2 Kwa kuwa kanuni ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imenifanya mimi
kuwa huru mbali na kanuni ya dhambi na mauti. 3 Kwa maana kile ambacho
sheria ilishindwa kufanya kwa sababu ilikuwa dhaifu katika mwili, Mungu alifanya.
Alimtuma Mwana wake wa pekee kwa mfano wa mwili wa dhambi awe sadaka
ya dhambi, na akaihukumu dhambi katika mwili. 4 Alifanya hivi ili maagizo ya
sheria yatimilizwe ndani yetu, sisi tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali
kwa kufuata mambo ya Roho. 5 Wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili,
lakini wale waifuatao Roho huyafikiri mambo ya Roho. 6 Kwa kuwa nia ya mwili
ni mauti, bali nia ya Roho ni uzima na amani. 7 Hii ni kwa sababu ile nia ya mwili
ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii.
8 Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu. 9 Hata hivyo, hampo katika
mwili bali katika Roho, kama ni kweli kwamba Roho wa Mungu huishi ndani yenu.
Lakini kama mtu hana Roho wa Kristo, yeye si wake. 10 Kama Kristo yumo ndani
yenu, mwili umekufa kwa mambo ya dhambi, bali roho ni hai kwa mambo ya haki.
11 Ikiwa Roho wa yule aliyemfufua Yesu kutoka wafu huishi ndani yenu, yeye yule
aliyemfufua Kristo kutoka katika wafu ataipa pia miili yenu ya mauti uhai kwa njia
ya Roho wake, aishie ndani yenu. 12 Hivyo basi, ndugu zangu, sisi tu wadeni, lakini
si kwa mwili kwamba tuishi kwa jinsi ya mwili. 13 Maana ikiwa mnaishi kwa jinsi ya
mwili, mpo karibu kufa, lakini ikiwa kwa Roho mnayafisha matendo ya mwili, nanyi
mtaishi. 14 Maana kama ambavyo wengi wanaongozwa na Roho wa Mungu, hawa ni
wana wa Mungu. 15 Kwa kuwa hamkupokea roho wa utumwa tena hata muogope.
Badala yake, mlipokea roho ya kufanywa kuwa wana, ambayo kwayo tunalia, “Abba,
Baba!” 16 Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu ya kuwa tu watoto wa
Mungu. 17 Ikiwa tu watoto, basi tu warithi pia, warithi wa Mungu. Na sisi tu warithi
pamoja na Kristo, ikiwa kwa kweli tunateseka na yeye ili tupate kutukuzwa pamoja

naye. 18 Kwa kuwa nayahesabu mateso ya wakati huu kuwa si kitu nikilinganisha
na utukufu utakaofunuliwa kwetu. 19 Kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia
kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu. 20 Kwa maana uumbaji pia
ulitiishwa chini ya ubatili, si kwa hiari yake, ila kwa sababu yake yeye aliyevitiisha.
Ni katika tumaini 21 kwamba uumbaji wenyewe nao utawekwa huru na kutolewa
katika utumwa wa uharibifu, na kuingizwa katika uhuru wa utukufu wa watoto wa
Mungu. 22 Kwa maana twajua ya kuwa uumbaji nao pia unaugua na kuteseka kwa
uchungu pamoja hata sasa. 23 Si hivyo tu, ila na sisi wenyewe tulio na malimbuko ya
Roho - sisi pia tunaugua katika nafsi zetu, tukisubiri kufanywa wana, yaani ukombozi
wa miili yetu. 24 Kwa maana ni kwa taraja hili tuliokolewa. Lakini kitu kilichotarajiwa
kikionekana hakuna taraja tena, kwa maana ni nani anayekitarajia kile akionacho?
25 Bali tukikitarajia kitu tusichokiona, twakingojea kwa saburi. 26 Kwa jinsi iyo
hiyo, Roho naye hutusaidia katika udhaifu wetu. Kwa maana hatujui kuomba jinsi
itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa.
27 Na yeye aichunguzaye mioyo huijua akili ya Roho, kwa sababu huomba kwa
niaba yao walioamini kulingana na mapenzi ya Mungu. 28 Nasi twajua ya kuwa
kwa wote wampendao Mungu, yeye hufanya mambo yote pamoja kwa wema, kwa
wale wote walioitwa kwa kusudi lake. 29 Kwa sababu wale wote aliowajua tangu
asili, pia aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye
awe mzaliwa wa kwanza miogoni mwa ndugu wengi. 30 Na wale aliowachagua
tangu asili, hao aliwaita pia. Na wale aliowaita, hao aliwahesabia haki. Na wale
aliowahesabia haki, hao pia akawatukuza. 31 Tuseme nini basi juu ya mambo haya?
Mungu akiwa upande wetu, ni nani aliye juu yetu? 32 Yeye asiyemwachilia mwana
wake mwenyewe bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote atakosaje kutukirimia na mambo
yote pamoja naye? 33 Ni nani atakayewashitaki wateule wa Mungu? Mungu ndiye
mwenye kuwahesabia haki. 34 Ni nani atakayewahukumia adhabu? Kristo Yesu ndiye
aliyekufa kwa ajili yetu, na zaidi ya hayo, yeye pia alifufuliwa. Naye anatawala
pamoja na Mungu mahali pa heshima, na tena ndiye anayetuombea sisi. 35 Ni nani
atakayetutenga na upendo wa Kristo? Dhiki, au shida, au mateso, au njaa, au uchi,
au hatari, au upanga? 36 Kama ilivyoandikwa, “Kwa faida yako tunauawa mchana
kutwa. Tulihesabiwa kama kondoo wa kuchinjwa.” 37 Katika mambo haya yote sisi tu
zaidi ya washindi katika yeye aliyetupenda. 38 Kwa maana nimekwisha kushawishika
kwamba wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala mamlaka, wala vitu vilivyopo,
wala vitu vijavyo, wala nguvu, 39 wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe
kinginecho chote, hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu, ambaye ni Kristo
Yesu Bwana wetu.

# 9

1 Nasema ukweli katika Kristo. Sisemi uongo, na dhamira yangu hushuhudia
pamoja nami katika Roho Mtakatifu, 2 kwamba kuna huzuni kubwa na maumivu
yasiyo koma ndani ya moyo wangu. 3 Kwamba ningetamani mimi mwenyewe
kulaaniwa na kutengwa mbali na Kristo kwa ajili ya ndugu zangu, wale wa jamii
yangu katika mwili. 4 Wao ni Waisraeli. Walio na hali ya kufanyika watoto, wa
utukufu, wa maagano, na zawadi ya sheria, kumwabudu Mungu, na ahadi. 5 Wao ni
watangulizi ambako Kristo amekuja kwa heshima kuvaa mwili huu - ambaye yeye ni
Mungu wa vyote. Naye asifiwe milele. Amina. 6 Lakini si kwamba ahadi za Mungu
zimeshindwa kutimia. Maana si kila mtu aliye Israeli ni Mwiisraeli halisi. 7 Sivyo
hata kwa uzao wa Abrahamu kuwa ni watoto wake halisi. Lakini, “ni kupitia Isaka
uzao wako utaitwa.” 8 Hii ni kwamba, watoto wa mwili si watoto wa Mungu. Lakini
watoto wa ahadi wanatazamwa kuwa kama uzao. 9 Maana hili ndilo neno la ahadi:

“Katika majira haya nitakuja, na Sara atapewa mtoto.” 10 Si hili tu, lakini baada ya
Rebeka kupata mimba kwa mtu mmoja, Isaka baba yetu- 11 kwamba watoto walikuwa
bado hawajazaliwa na alikuwa hajafanya jambo lolote zuri au baya, ili kwamba
kusudi la Mungu kulingana na uchaguzi lisimame, wala si kwa matendo, lakini
ni kwa sababu ya yule aitae. 12 Ilinenwa kwake, “Mkubwa atamtumikia mdogo.”
13 Kama ilivyo kwisha andikwa: “Yakobo nilimpenda, lakini Esau nilimchukia.”
14 Basi tena tutasema nini? Je kuna udhalimu kwa Mungu? La hasha. 15 Kwa
kuwa anasema kwa Musa, “nitakuwa na rehema kwa yule nitakayemrehemu, na
nitakuwa na huruma kwa yule nitakayemhurumia.” 16 Kwa hiyo basi, si kwa sababu
ya yeye atakaye, wala si kwa sababu ya yeye ambaye hukimbia, lakini kwa sababu ya
Mungu, ambaye huonesha rehema. 17 Kwa kuwa maandiko husema kwa Farao, “Kwa
kusudi hili maalumu nilikuinua, ili kwamba nioneshe nguvu zangu katika wewe, na
ili kwamba jina langu litangazwe katika nchi yote.” 18 Hivyo basi, Mungu huwa na
rehema kwa yeyote ampendaye, na kwa ambaye humpenda, humfanya kuwa mkaidi.
19 Kisha utasema kwangu, “Kwa nini bado anaona kosa? Ni yupi ambaye alikwisha
kustahimili matakwa yake?” 20 Kinyume chake, mwanadamu, wewe ni nani ujibue
kinyume na Mungu? Kuna uwezekano wowote wa kilichofinyangwa kusema kwa
mfinyanzi, “Kwanini ulinifanya hivi mimi?” 21 Je mfinyazi huwa hana haki juu ya
udongo kutengeneza chombo kwa matumizi maalumu kutokana na bonge lile lile,
na chombo kingine kwa matumizi ya kila siku? 22 Vipi kama Mungu, ambaye ana
utayari wa kuonesha gadhabu yake na kufanya nguvu yake kujulikana, alistahimili
kwa uvumilivu wa kutosha vyombo vya gadhabu vilivyoandaliwa kwa kuangamiza?
23 Vipi kama alifanya hivi ili kwamba aoneshe wingi wa utukufu wake juu ya vyombo
vya rehema, ambavyo alikwisha kuviandaa kwa ajili ya utukufu? 24 Vipi kama
alifanya hii pia kwetu, ambaye pia alituita, si tu kutoka kwa Wayahudi, lakini pia
kutoka kwa watu wa Mataifa? 25 Kama asemavyo pia katika Hosea: “Nitawaita watu
wangu ambao hawakuwa watu wangu, na mpendwa wake ambaye hakupendwa.
26 Na itakuwa kwamba pale iliposemwa kwao, 'Ninyi si watu wangu,' pale wataitwa
'wana wa Mungu aliye hai.”' 27 Isaya analia kuhusiana na Israeli, “Kama hesabu
ya wana wa Israeli ingekuwa kama mchanga wa bahari, itakuwa ni masalia ambao
wataokolewa. 28 Kwa kuwa Bwana atalichukua neno lake juu ya nchi, mapema na
kwa utimilifu. 29 Na kama jinsi Isaya alivyosema awali, “Kama Bwana wa majeshi
hakutuachia nyuma uzao kwa ajili yetu, tungekuwa kama Sodoma, na tungefanywa
kama Gomora. 30 Tutasema nini basi? kwamba watu wa Mataifa ambao walikuwa
hawatafuti haki, walipata haki, haki kwa imani. 31 Lakini Israeli, ambaye alitafuta
sheria ya haki, hakuifikia. 32 Kwanini si hivyo? Kwa sababu hawakuitafuta kwa
imani, bali kwa matendo. Walijikwaa juu ya jiwe la kujikwaa, 33 kama ilivyo kwisha
andikwa, “Tazama, nimelaza jiwe la kujikwaa katika Sayuni na mwamba wa kukosa.
Yeye ambaye huamini katika hili hataaibika.”

# 10

1 Ndugu, nia ya moyo wangu na ombi langu kwa Mungu ni kwa ajili yao, kwa
ajili ya wokovu wao. 2 Kwa kuwa nawashuhudia kwamba wanajuhudi kwa ajili ya
Mungu, lakini si kwa ajili ya ufahamu. 3 Kwa kuwa hawajui haki ya Mungu, na
wanatafuta kujenga haki yao wenyewe. Hawakuwa watiifu kwa haki ya Mungu.
4 Kwa kuwa Kristo ndiye utimilifu wa sheria kwa ajili ya haki ya kila mtu aaminiye.
5 Kwa kuwa Musa anaandika kuhusu haki ambayo huja kutokana na sheria: “Mtu
ambaye hutenda haki ya sheria ataishi kwa haki hii.” 6 Lakini haki ambayo inatokana
na imani husema hivi, “Usiseme moyoni mwako, 'Nani atapaa kwenda mbinguni?'
(Hii ni kumleta Kristo chini). 7 Na usiseme, 'Nani atashuka katika shimo?”' (Hii ni,

kumleta Kristo juu kutoka kwa wafu). 8 Lakini inasema nini? “Neno liko karibu na
wewe, katika kinywa chako na katika moyo wako.” Hilo ni neno la imani, ambalo
tunatangaza. 9 Kwa kuwa kama kwa kinywa chako unamkiri Yesu ya kuwa ni
Bwana, na kuamini moyoni mwako kwamba Mungu alimfufua kutoka kwa wafu,
utaokoka. 10 Kwa kuwa kwa moyo mtu huamini na kupata haki, na kwa kinywa
hukiri na kupata wokovu. 11 Kwa kuwa andiko lasema, “Kila amwaminiye hata
aibika.” 12 kwa kuwa hakuna tofauti kati ya Myahudi na Myunani. Kwa kuwa Bwana
yule yule ni Bwana wa wote, na ni tajiri kwa wote wamwitao. 13 Kwa kuwa kila
mtu ambaye huliitia jina la Bwana ataokoka. 14 Kwa jinsi gani wanaweza kumwita
yeye ambaye hawajamwamini? Na jinsi gani wanaweza kuamini katika yeye ambaye
hawajamsikia? Na watasikiaje pasipo muhubiri? 15 Na jinsi gani wanaweza kuhubiri,
isipokuwa wametumwa? - Kama ilivyoandikwa, “Jinsi gani ni mizuri miguu ya
wale ambao wanatangaza habari za furaha za mambo mema!” 16 Lakini wote
hawakusikiliza injili. Kwa kuwa Isaya hunena, “Bwana, ni nani aliyesikia ujumbe
wetu?” 17 Hivyo imani huja kutokana na kusikia, na kusikia kwa neno la Kristo.
18 Lakini nasema, “Je hawakusikia?” Ndiyo, kwa hakika sana. “Sauti yao imekwisha
toka nje katika nchi yote, na maneno yao kwenda miisho ya dunia.” 19 Zaidi ya
yote, Ninasema, “Je Israel hakujua?” Kwanza Musa hunena, “Nitawachokoza kuwatia
wivu kwa watu ambao si taifa. Kwa njia ya taifa lisilo na uelewa, nitawachochea
hadi mkasirike.” 20 Na Isaya ni jasiri sana na husema, “Nilipatikana na wale ambao
hawakunitafuta. Nilionekana kwa wale ambao hawakunihitaji.” 21 Lakini kwa Israel
husema, “Siku zote nilinyoosha mikono yangu kwa wasiotii na kwa watu wagumu.”

# 11

1 Basi nasema, je, Mungu aliwakataa watu wake? Hata kidogo. Kwa kuwa mimi pia
ni Mwiisraeli, wa ukoo wa Abrahamu, wa kabila la Benyamini. 2 Mungu hakuwakataa
watu wake, aliowajua tangu mwanzo. Je hamjui andiko linasema nini kuhusu Eliya,
jinsi alivyomsihi Mungu juu ya Israeli? 3 “Bwana, wamewaua manabii wako, nao
wamebomoa madhabahu zako. Mimi peke yangu nimesalia, nao wanatafuta uhai
wangu.” 4 Lakini jibu la Mungu lasema nini kwako? “Nimetunza kwa ajili yangu
watu elfu saba ambao hawampigii magoti Baali.” 5 Hata hivyo, wakati huu wa sasa
pia kuna walio salia kwa sababu ya uchaguzi wa neema. 6 Lakini ikiwa ni kwa
neema, si tena kwa matendo. Vinginevyo neema haitakuwa tena neema. 7 Ni nini
basi? Jambo ambalo Israeli alikuwa akitafuta, hakukipata, bali wateule walikipata,
na wengine walitiwa uzito. 8 Ni kama ilivyoandikwa: “Mungu amewapa roho ya
ubutu, macho ili wasione, na masikio ili wasisikie, mpaka leo hii.” 9 Naye Daudi
anasema, “Acha meza zao na ziwe wavu, mtego, sehemu ya kujikwaa, na kulipiza
kisasi dhidi yao. 10 Acha macho yao yatiwe giza ili wasiweze kuona. Ukawainamishe
migongo yao daima.” 11 Basi nasema, “Je, wamejikwaa hata kuanguka?” Isiwe hivyo
kamwe. Badala yake, kwa kushindwa kwao, wokovu umefika kwa Mataifa, ili wao
wenyewe watiwe wivu. 12 Sasa ikiwa kushindwa kwao ni utajiri wa ulimwengu, na
kama hasara yao ni utajiri wa mataifa, ni kiasi gani zaidi itakuwa kukamilika kwao?
13 Na sasa naongea nanyi watu wa Mataifa. Kwa kuwa nimekuwa mtume kwa watu
wa Mataifa mengine, najivunia huduma yangu. 14 Labda nitawatia wivu walio mwili
mmoja na mimi. Labda tutawaokoa baadhi yao. 15 Maana ikiwa kukataliwa kwao ni
maridhiano ya dunia, kupokelewa kwao kutakuwaje ila uhai toka kwa wafu? 16 Kama
matunda ya kwanza ni akiba, ndivyo ilivyo kwa donge la unga. Kama mzizi ni akiba,
matawi nayo kadhalika. 17 Lakini kama baadhi ya matawi yamekatwa, kama wewe,
tawi pori la mzeituni, ulipandikizwa kati yao, na kama ulishiriki pamoja nao katika
mizizi ya utajiri wa mzeituni, 18 usijisifu juu ya matawi. Lakini kama unajisifu, si

wewe ambaye unaisaidia mizizi, bali mizizi inakusaidia wewe. 19 Basi utasema,
“Matawi yalikatwa ili nipate kupandikizwa katika shina.” 20 Hiyo ni kweli. Kwa
sababu ya kutoamini kwao walikatwa, lakini wewe ulisimama imara kwa sababu ya
imani yako. Usijifikirie mwenyewe kwa hali ya juu sana, bali ogopa. 21 Kwa maana
ikiwa Mungu hakuyaachia matawi ya asili, hatakuhurumia wewe pia. 22 Angalia,
basi, matendo mema na ukali wa Mungu. Kwa upande mmoja, ukali ulikuja juu ya
Wayahudi ambao walianguka. Lakini kwa upande mwingine, wema wa Mungu huja
juu yako, kama utadumu katika wema wake. Vinginevyo wewe pia utakatiliwa mbali.
23 Na pia, kama hawataendelea katika kutoamini kwao, watapandikizwa tena. Maana
Mungu anao uwezo wa kuwapandikiza tena. 24 Kwa maana ikiwa ninyi mlikatwa
nje kwa ulio kwa asili mzeituni mwitu, na kinyume cha asili mlipandikizwa katika
mzeituni ulio mwema, si zaidi sana hawa Wayahudi, ambao ni kama matawi ya asili
kuweza kupandikizwa tena ndani ya mzeituni wao wenyewe? 25 Kwa maana ndugu
sitaki msijue, kuhusiana na siri hii, ili kwamba msiwe na hekima katika kufikiri
kwenu wenyewe. Siri hii ni kwamba ugumu umetokea katika Israeli, hadi kukamilika
kwa mataifa kutakapokuja. 26 Hivyo Israeli wote wataokoka, kama ilivyoandikwa:
“Kutoka Sayuni atakuja Mkombozi. Atauondoa uovu kutoka kwa Yakobo. 27 Na hili
litakuwa agano langu pamoja nao, wakati nitakapoziondoa dhambi zao.” 28 Kwa
upande mmoja kuhusu injili, wanachukiwa kwa sababu yenu. Kwa upande mwingine
kutokana na uchaguzi wa Mungu, wamependwa kwa sababu ya mababu. 29 Kwa
kuwa zawadi na wito wa Mungu haubadiliki. 30 Kwa kuwa awali ninyi mlikuwa
mmemwasi Mungu, lakini sasa mmeipokea rehema kwa sababu ya kuasi kwao.
31 Kwa njia iyo hiyo, sasa hawa Wayahudi wameasi. Matokeo yake ni kwamba
kutokana na huruma mliyojaliwa ninyi wanaweza pia kupokea rehema. 32 Maana
Mungu amewafunga watu wote katika uasi, ili aweze kuwahurumia wote. 33 Jinsi
zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! Hazichunguziki hukumu zake,
na njia zake hazigunduliki! 34 “Maana ni nani aliyeijua nia ya Bwana? Au ni nani
amekuwa mshauri wake? 35 Au ni nani kwanza aliyempa kitu Mungu, ili alipwe
tena?” 36 Kwa maana kutoka kwake, na kwa njia yake na kwake, vitu vyote vipo.
Kwake uwe utukufu milele. Amina.

# 12

1 Kwa hiyo nawasihi, ndugu, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe
dhabihu iliyo hai, takatifu, inayokubalika kwa Mungu. Hii ndiyo ibada yenu yenye
maana. 2 Wala msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya
nia zenu. Fanyeni hivi mpate kujua mapenzi ya Mungu yaliyo mema, yakumpendeza
na kamilifu. 3 Kwa maana nasema, kwa sababu ya neema niliyopewa, kwamba
kila mtu ambaye yupo miongoni mwenu hapaswi kufikiri zaidi juu yake mwenyewe
kuliko inavyompasa kufikiri. Bali, imempasa kufikiri kwa hekima, kama ambavyo
Mungu amewapa kila mmoja kiasi fulani cha imani. 4 Kwa kuwa tuna viungo vingi
katika mwili mmoja, lakini si viungo vyote vina kazi moja. 5 Vivyo hivyo, sisi
tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, na viungo kila mmoja kwa mwenzake.
6 Tuna karama zilizo mbalimbali kwa kadiri ya neema mliyopewa. Ikiwa karama
ya mtu ni unabii, na itendeke kwa kadiri ya imani yake. 7 Ikiwa karama ya mtu ni
huduma, na atumike. Ikiwa mwingine ana karama ya kufundisha, basi, afundishe.
8 Ikiwa karama ya mtu ni faraja, basi, afariji. Ikiwa karama ya mtu ni kutoa,
afanye hivyo kwa ukarimu. Ikiwa karama ya mtu ni kuongoza, na litendeke kwa
uangalifu. Ikiwa karama ya mtu ni katika kuonesha huruma, na litendeke kwa
furaha. 9 Pendo lisiwe na unafiki. Chukieni uovu; mshikilie yaliyo mema. 10 Kuhusu
upendo wa ndugu, pendaneni ninyi kwa ninyi. Kuhusu heshima, heshimianeni

ninyi kwa ninyi. 11 Kuhusu bidii, msiwe walegevu. Kuhusu roho, iweni na shauku.
Kuhusu Bwana, mtumikieni. 12 Furahini katika ujasiri mlionao kuhusu siku zijazo.
Muwe na subira katika matatizo yenu. Mdumu katika kuomba. 13 Mshiriki katika
mahitaji ya waumini. Tafuteni njia nyingi za kuonesha ukarimu. 14 Watakieni baraka
wote wanaowatesa ninyi; muwabariki na wala msiwalaani. 15 Furahini pamoja na
wanaofurahi, lieni pamoja na wanaolia. 16 Muwe na nia moja ninyi kwa ninyi.
Msifikiri kwa kujivuna, lakini wakubalini watu wa hali ya chini. Msiwe na hekima
juu ya mawazo yenu wenyewe. 17 Msimlipe mtu yeyote ovu kwa ovu. Fanyeni
mambo mema machoni pa watu wote. 18 Kama inawezekana, kama ilivyowekwa
kwenu, muwe na amani na watu wote. 19 Wapenzi, msijilipizie kisasi wenyewe,
lakini ipisheni ghadhabu ya Mungu. Kwa maana imeandikwa, '' 'kisasi ni changu;
Mimi nitalipa,' asema Bwana." 20 "Lakini ikiwa adui yako ana njaa, mlishe. Akiwa
na kiu, mnyweshe. Kwa maana ukifanya hivyo, utampalia makaa ya moto juu ya
kichwa chake." 21 Usishindwe na ubaya, bali ushinde ubaya kwa wema.

## 13

1 Kila nafsi na iwe na utii kwa mamlaka ya juu, kwa kuwa hakuna mamlaka
isipokuwa imetoka kwa Mungu. Na mamlaka zilizopo zimewekwa na Mungu. 2 Kwa
hiyo ambaye anapinga mamlaka hiyo hupinga amri ya Mungu; na wale waipingao
watapokea hukumu juu yao wenyewe. 3 Kwa kuwa watawala si tishio kwa watendao
mema, bali kwa watendao maovu. Je unatamani kutoogopa mamlaka? Fanya yaliyo
mema, na utasifiwa nayo. 4 Kwa kuwa ni mtumishi wa Mungu kwako kwa ajili ya
mema. Bali kama utatenda yaliyo maovu, ogopa; kwa kuwa habebi upanga bila
sababu. Kwa kuwa ni mtumishi wa Mungu, mlipa kisasi kwa ghadhabu juu ya yule
afanyaye uovu. 5 Kwa hiyo inakupasa utii, si tu kwa sababu ya gadhabu, bali pia kwa
sababu ya dhamiri. 6 Kwa ajili hii pia unalipa kodi. Kwa kuwa wenye mamlaka ni
watumishi wa Mungu, ambao wanaendelea kufanya jambo hili. 7 Mlipeni kila mmoja
ambacho wanawadai: kodi kwa astahiliye kodi; ushuru kwa astahiliye ushuru; hofu
kwa astahiliye hofu; heshima kwa astahiliye heshima. 8 Msidaiwe na mtu kitu
chochote, isipokuwa kupendana ninyi kwa ninyi. Kwa kuwa yeye ampendaye jirani
yake ametimiliza sheria. 9 Kwa kuwa, "Hautazini, hautaua, hautaiba, hautatamani,"
na kama kuna amri nyingine pia, imejumlishwa katika sentensi hii: "Utampenda
jirani yako kama wewe mwenyewe." 10 Upendo hamdhuru jirani wa mtu. Kwa hiyo,
upendo ni ukamilifu wa sheria. 11 Kwa sababu ya hili, mnajua wakati, kwamba tayari
ni wakati wa kutoka katika usingizi. Kwa kuwa wokovu wetu umekaribia zaidi ya
wakati ule tulio amini kwanza. 12 Usiku umeendelea, na mchana umekaribia. Na
tuweke pembeni matendo ya giza, na tuvae silaha za nuru. 13 Na tuenende sawa
sawa, kama katika nuru, si kwa sherehe za uovu au ulevi. Na tusienende katika
zinaa au tamaa isiyoweza kudhibitiwa, na si katika fitina au wivu. 14 Bali tumvae
Bwana Yesu Kristo, na tusiweke nafasi kwa ajili ya mwili, kwa tamaa zake.

## 14

1 Mpokeeni yeyote ambaye ni dhaifu katika imani, bila kutoa hukumu kuhusu
mawazo yake. 2 Mtu mmoja ana imani ya kula chochote, mwingine ambaye ni
dhaifu anakula mboga tu. 3 Mtu ambaye anakula kila kitu asimdharau yeye asiyekula
kila kitu. Na yeye ambaye hali kila kitu asimuhukumu mwingine ambaye hula
kila kitu. Kwa kuwa Mungu amekwisha mpokea. 4 Wewe ni nani, wewe ambaye
unamuhukumu mtumishi ambaye ni miliki ya mtu mwingine? Ni mbele ya Bwana
wake kwamba husimama au huanguka. Lakini atainuliwa, kwa kuwa Bwana
anaweza kumfanya asimame. 5 Mtu mmoja huthamini siku moja kuliko nyingine.

Mwingine huthamini kila siku sawa sawa. Hebu kila mtu na ashawishike katika
akili yake mwenyewe. 6 Yeye ambaye anashika siku, anashika kwa ajili ya Bwana.
Na kwa yeye alaye, hula kwa ajili ya Bwana, kwa kuwa anampa Mungu shukrani.
Yeye ambaye hali, hujizuia kutokula kwa ajili ya Bwana. Yeye pia hutoa shukrani
kwa Mungu. 7 Kwa kuwa hakuna aishie kwa nafsi yake, na hakuna afae kwa ajili
yake mwenyewe. 8 Kwa kuwa ikiwa tunaishi, tunaishi kwa ajili ya Bwana. Na ikiwa
tunakufa, tunakufa kwa ajili ya Bwana. Basi ikiwa tunaishi au tunakufa tu mali
ya Bwana. 9 Kwa kuwa ni kwa kusudi hili Kristo alikufa na kuishi tena, kwamba
awe Bwana wa wote wafu na waishio. 10 Lakini wewe, kwa nini unamuhukumu
ndugu yako? Na wewe, kwa nini unamdharau ndugu yako? Kwa kuwa sisi sote
tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu. 11 Kwa kuwa imeandikwa, "Kama
niishivyo," asema Bwana, "Kwangu mimi kila goti litapigwa, na kila ulimi utatoa sifa
kwa Mungu." 12 Hivyo basi, kila mmoja wetu atatoa hesabu yake mwenyewe kwa
Mungu. 13 Kwa hiyo, tusiendelee tena kuhukumiana, lakini badala yake amua hivi,
kwamba hakuna atakaye weka kikwazo au mtego kwa ndugu yake. 14 Ninajua na
nimeshawishika katika Bwana Yesu, kwamba hakuna kitu kilicho najisi chenyewe.
Ni kwa yeye tu anayedhani kuwa chochote ni najisi, kwa kuwa kwake ni najisi.
15 Ikiwa kwa sababu ya chakula ndugu yako anahuzunika, hautembei tena katika
upendo. Usimharibu kwa chakula chako mtu ambaye kwa ajili yake Kristo alikufa.
16 Hivyo msiruhusu matendo yenu mema yakasababisha watu kuwadhihaki. 17 Kwa
kuwa ufalme wa Mungu si kwa ajili ya chakula na kinywaji, bali ni kwa ajili ya
haki, amani, na furaha katika Roho Mtakatifu. 18 Kwa kuwa yeye amtumikiaye
Kristo kwa jinsi hii amekubalika kwa Mungu na amekubalika kwa watu. 19 Kwa hiyo
basi, na tufuate mambo ya amani na mambo ambayo humjenga mtu na mwingine.
20 Usiharibu kazi ya Mungu kwa sababu ya chakula. Vitu vyote kwa kweli ni
safi, lakini ni vibaya kwa mtu yule ambaye hula na kumsababisha yeye kujikwaa.
21 Ni vyema kutokula nyama, wala kunywa divai, wala chochote ambacho kwa
hicho ndugu yako hukwazwa. 22 Hizi imani maalumu ulizo nazo, ziweke kati yako
mwenyewe na Mungu. Amebalikiwa yule ambaye hajihukumu mwenyewe katika
kile anachokikubali. 23 Aliye na mashaka amehukumiwa ikiwa anakula, kwa sababu
haitokani na imani. Na chochote kisichotokana na imani ni dhambi.

# 15

1 Sasa sisi tulio na nguvu tunapaswa kuuchukua udhaifu wa walio dhaifu, na
hatupaswi kujipendeza wenyewe. 2 Kila mmoja wetu ampendeze jirani yake kwani ni
jambo jema, kwa lengo la kumjenga. 3 Kwani hata Kristo hakujipendeza mwenyewe.
Badala yake, ilikuwa kama ilivyoandikwa, "Matusi ya wale waliokutukana ya-
menipata mimi." 4 Kwa chochote kilichotangulia kuandikwa, kiliandikwa kwa
kutuelekeza, kwa kusudi kwamba kupitia uvumilivu na kupitia kutiwa moyo na
maandiko tungekuwa na ujasiri. 5 Sasa Mungu wa uvumilivu na wa kutia moyo
awape kuwa na nia sawa kwa kila mmoja kulingana na Yesu Kristo. 6 Aweze
kufanya hivi kwa nia moja muweze kumsifu kwa kinywa kimoja Mungu na Baba
wa Bwana wetu Yesu Kristo. 7 Kwa hiyo mpokeeni kila mmoja, kama vile Kristo
alivyowapokea, kwa utukufu wa Mungu. 8 Kwani nasema kwamba Kristo amefanywa
mtumishi wa tohara kwa niaba ya ukweli wa Mungu. Alifanya hivi ili kwamba
aweze kuthibitisha ahadi zilizotolewa kwa mababa, 9 na kwa mataifa kumtukuza
Mungu kwa neema yake. Kama ambavyo imeandikwa, "Kwa hiyo nitatoa sifa
kwako miongoni mwa mataifa na kuimba sifa katika jina lako." 10 Tena inasema,
"Furahini, ninyi watu wa mataifa, pamoja na watu wake." 11 Na tena, "Msifuni
Bwana, ninyi mataifa yote; acha watu wa mataifa yote wamsifu yeye." 12 Tena

Isaya asema, “Kutakuwa na shina la Yese, na mmoja atakayeinuka kutawala juu ya
mataifa. Mataifa watakuwa na tumaini katika yeye.” 13 Sasa Mungu wa tumaini
awajaze na furaha yote na amani kwa kuamini, ili kwamba muweze kuzidi katika
tumaini, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. 14 Mimi mwenyewe pia nimeshawishiwa
nanyi, ndugu zangu. Nimeshawishiwa kwamba pia ninyi wenyewe mmejazwa na
wema, mmejazwa na maarifa yote. Ninashawishiwa kwamba, ninyi mwaweza pia
kuhimizana kila mmoja na mwenzake. 15 Lakini ninaandika kwa ujasiri zaidi kwenu
juu ya mambo fulani ili kuwakumbusha tena, sababu ya kipawa nilichopewa na
Mungu. 16 Kipawa hiki kilikuwa kwamba niweze kuwa mtumishi wa Yesu Kristo
aliyetumwa kwa mataifa, kujitoa kama kuhani wa injili ya Mungu. Ningeweza
kufanya hivi ili kujitoa kwangu kwa mataifa kuwe kumekubaliwa, kumetengwa
na Mungu kwa njia ya Roho Mtakatifu. 17 Hivyo furaha yangu iko katika Kristo
Yesu na katika mambo ya Mungu. 18 Kwani sitaweza kuthubutu kunena lolote
isipokuwa kwamba Kristo amekamilisha kupitia kwangu utii wa mataifa. Haya
mambo yametimizwa kwa neno na tendo, 19 kwa nguvu za ishara na maajabu, na kwa
nguvu za Roho Mtakatifu. Hii ilikuwa ili kwamba kutoka Yerusalem, na kuzungukia
mbali kama Iliriko, niweze kuichukua nje kwa ukamilifu injili ya Kristo. 20 Kwa
njia hii, nia yangu imekuwa kuitangaza injili, lakini si mahali Kristo anajulikana
kwa jina, ili kwamba nisiweze kujenga juu ya msingi wa mtu mwingine. 21 Kama
ilivyoandikwa: “Ambao kwa yeye hawana habari zake alikuja watamwona, na wale
ambao hawakumsikia watamfahamu.” 22 Kwahiyo nilikuwa pia nimezuiliwa mara
nyingi kuja kwenu. 23 Lakini sasa, sina tena sehemu yoyote katika mikoa hii, na
nimekuwa nikitamani kwa miaka mingi kuja kwenu. 24 Hivyo mara zote nikienda
Hispania, ninatumaini kuwaona nikipita, na kuweza kupelekwa njia yangu na ninyi,
baada ya kuwa nimefurahia ushirika na ninyi kwa muda. 25 Lakini sasa ninakwenda
Yerusalemu kuwahudumia waumini. 26 Maana iliwapendeza watu wa Makedonia
na Akaya kufanya changizo maalumu kwa masikini miongoni mwa waumini huko
Yerusalemu. 27 Ndiyo, ilikuwa kwa upendo wao, na hakika, wamekuwa wadeni wao.
Maana ikiwa mataifa wameshiriki katika mambo yao ya kiroho, wanadaiwa na wao
pia kuwahudumia katika mahitaji ya vitu. 28 Kwahiyo, wakati nimekamilisha hivi
na kuwa na utoshelevu wa tunda hili kwao, mimi nitakwenda njiani pamoja nanyi
huko Hispania. 29 Najua kwamba, wakati nikija kwenu, nitakuja katika utimilifu wa
baraka za Kristo. 30 Sasa ninawasihi, ndugu, kwa Bwana wetu Yesu Kristo, na kwa
upendo wa Roho, kwamba mshiriki pamoja nami katika maombi yenu kwa Mungu
kwa ajili yangu. 31 Ombeni kwamba niweze kuokolewa kutoka kwao wasio na utii
katika Yudea, na kwamba huduma yangu huko Yerusalemu iweze kupokelewa na
waumini. 32 Ombeni kwamba ninaweza kuja kwenu kwa furaha kupitia mapenzi ya
Mungu, na kwamba niweze kuwa pamoja nanyi, kupata kupumzika. 33 Na Mungu
wa amani awe pamoja nanyi nyote. Amina

# 16

1 Namkabidhi kwenu Fibi dada yetu, ambaye ni mtumishi wa kanisa ambalo liko
Kenkrea, 2 ili kwamba mnaweza kumpokea katika Bwana. Fanyeni hivi katika
kicho cha thamani cha waumini, na msimame pamoja naye katika jambo lolote
atakalokuwa na uhitaji nalo. Maana yeye mwenyewe amekuwa mhudumu wa wengi,
na kwa ajili yangu mwenyewe. 3 Msalimu Priska na Akila, watenda kazi pamoja
nami katika Kristo Yesu, 4 ambao kwa maisha yangu waliyahatarisha maisha yao
wenyewe. Ninatoa shukrani kwao, na siyo tu mimi, bali pia kwa makanisa yote
ya mataifa. 5 Lisalimie kanisa ambalo liko nyumbani kwao. Msalimie Epanieto
mpendwa wangu, ambaye ni mzaliwa wa kwanza wa Kristo katika Asia. 6 Msalimie

Mariamu ambaye ametenda kazi kwa bidii kwa ajili yenu. 7 Msalimie Androniko
na Yunia, jamaa zangu, na wafungwa pamoja nami. Ni wa muhimu miongoni mwa
mitume, ambao pia walitangulia kumjua Kristo kabla yangu. 8 Msalimie Ampliato,
mpendwa wangu katika Bwana. 9 Msalimie Urbano, mtenda kazi pamoja nami katika
Kristo, na Stakisi mpendwa wangu. 10 Msalimie Apele, mwenye kukubaliwa katika
Kristo. Wasalimie wote ambao walio katika nyumba ya Aristobulo. 11 Nisalimie
Herodioni, jamaa yangu. Nisalimie wote walio katika nyumba ya Narkiso, ambao
wako katika Bwana. 12 Nisalimie Trifaina na Trifosa, wanaotenda kazi kwa bidii
katika Bwana. msalimie Persisi mpendwa, ambaye ametenda kazi zaidi kwa Bwana,
13 Nisalimie Rufo, aliyechaguliwa katika Bwana na mama yake na wangu. 14 Msalimie
Asinkrito, Flegon, Herme, Patroba, Herma, na ndugu wote walio pamoja nao.
15 Nisalimie Filologo naYulia, Nerea na dada yake, na Olimpa, na waumini wote
walio pamoja nao. 16 Nisalimie kila mmoja kwa busu takatifu. Makanisa yote
katika Kristo yawasalimu. 17 Sasa nawasihi, ndugu, kutafakari juu ya hao ambao
wanasababisha mgawanyiko na vipingamizi. Wanakwenda kinyume na mafundisho
ambayo mmekwisha kujifunza. Geukeni mtoke kwao. 18 Kwa maana watu kama
hawa hawamtumikii Kristo Bwana, bali matumbo yao wenyewe. Kwa maneno yao
laini na pongezi za uongo wanadanganya mioyo ya wasio na hatia. 19 Kwa mfano
wa utii wenu mwamfikia kila mmoja. Kwa hiyo, nafurahi juu yenu, lakini nawataka
ninyi mwe na busara katika hali ya wema, na kutokuwa na hatia mbele ya uovu.
20 Mungu wa amani hatakawia kumwangamiza shetani chini ya nyayo zenu. Neema
ya Bwana Yesu Kristo iwe pamoja nanyi. 21 Timotheo, mtendakazi pamoja nami,
awasalimu, na Lukio, Yasoni na Sospeter, jamaa zangu. 22 Mimi, Tertio, niliyeuandika
waraka huu, nawasalimu katika jina la Bwana. 23 Gayo, aliyenitunza na kwa kanisa
lote, lawasalimu. Erasto, mtunza hazina wa mji, awasalimu, pamoja na Kwarto aliye
ndugu. 24 (Zingatia: Katika nakala halisi za kwanza, mstari huu haupo. Tazama
Warumi 16: 20. “Neema ya Bwana Yesu Kristo ikae nanyi nyote. Amina.”) 25 Sasa
kwake yeye aliye na uwezo kufanya msimame kulingana na injili na mafundisho ya
Yesu Kristo, kulingana na ufunuo wa siri iliyofichwa kwa muda mrefu, 26 lakini sasa
imekwisha funuliwa na kufanywa kujulikana na maandiko ya unabii kulingana na
amri ya Mungu wa milele, kwa utii wa imani miongoni mwa mataifa yote? 27 Kwa
Mungu pekee mwenye hekima, kupitia Yesu Kristo, kuwe na utukufu milele yote.
Amina

# 1 Wakorintho

1 Paulo, aliyeitwa na Kristo Yesu kuwa mtume kwa mapenzi ya Mungu, na Sosthene
ndugu yetu, 2 kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, kwa wale ambao wamewekwa
wakfu katika Yesu Kristo, ambao wameitwa kuwa watu watakatifu. Tunawaandikia
pia wale wote wanaoliitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo katika mahali pote, Bwana
wao na wetu. 3 Neema na amani iwe kwenu kutoka kwa Mungu baba yetu na Bwana
wetu Yesu Kristo. 4 Siku zote namshukru Mungu wangu kwa ajili yenu, kwa sababu
ya neema ya Mungu ambayo Kristo Yesu aliwapa. 5 Amewafanya kuwa matajiri
katika kila njia, katika usemi na pamoja maarifa yote. 6 Amewafanya matajiri,
kama ushuhuda kuhusu Kristo ya kwamba amethibitishwa kuwa kweli miongoni
mwenu. 7 Kwa hiyo hampungukiwi karama za kiroho, kama mlivyo na hamu ya
kusubiri ufunuo wa Bwana wetu Yesu Kristo. 8 Atawaimarisha ninyi pia hadi mwisho,
ili msilaumiwe siku ya Bwana wetu Yesu Kristo. 9 Mungu ni mwaminifu ambaye
aliwaita ninyi katika ushirika wa mwana wake, Yesu Kristo Bwana wetu. 10 Sasa
nawasihi kaka na dada zangu, kupitia jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba
wote mkubali, na kwamba kusiwe na migawanyiko miongoni mwenu. Nawasihi
kwamba muungane pamoja katika nia moja na katika kusudi moja. 11 Kwani watu
wa nyumba ya Kloe wamenitaarifu kuwa kuna mgawanyiko unaoendelea miongoni
mwenu. 12 Nina maana hii: Kila mmoja wenu husema, “Mimi ni wa Paulo,” au
“Mimi ni wa Apolo”, au “Mimi ni wa Kefa” au “Mimi ni wa Kristo”. 13 Je! Kristo
amegawanyika? Je! Paulo alisulubiwa kwa ajili yenu? Je! Mlibatizwa kwa jina la
Paulo? 14 Namshukuru Mungu kuwa sikumbatiza yeyote, isipokuwa Krispo na Gayo.
15 Hii ilikuwa kwamba hakuna yeyote angesema mlibatizwa kwa jina langu. 16 (Pia
niliwabatiza wa nyumba ya Stephania. Zaidi ya hapo, sijui kama nilimbatiza mtu
mwingine yeyote). 17 Kwa kuwa, Kristo hakunituma kubatiza bali kuhubiri injili.
Hakunituma kuhubiri kwa maneno ya hekima ya kibinadamu, ili kwamba nguvu ya
msalaba wa Kristo isiondolewe. 18 Kwa kuwa ujumbe wa msalaba ni upuuzi kwa wale
wanaokufa. Lakini kwa wale ambao Mungu anawaokoa, ni nguvu ya Mungu. 19 Kwa
kuwa imeandikwa, “Nitaiharibu hekima ya wenye busara. Nitauharibu ufahamu wa
wenye akili.” 20 Yuko wapi mtu mwenye busara? Yuko wapi mwenye elimu? Yuko
wapi msemaji mshawishi wa dunia hii? Je, Mungu hakuigeuza hekima ya dunia
hii kuwa ujinga? 21 Tangu dunia imekuwa katika hekima yake haikumjua Mungu,
ilimpendeza Mungu katika ujinga wao wa kuhubiri ili kuokoa wale wanaoamini.
22 Kwa Wayahudi huuliza ishara za miujiza na kwa Wayunani hutafuta hekima.
23 Lakini tunamhubiri Kristo aliyesulubiwa, aliye kikwazo kwa Wayahudi na ni
ujinga kwa Wayunani. 24 Lakini kwa wale ambao waliitwa na Mungu, Wayahudi
na Wayunani, tunamhubiri Kristo kama nguvu na hekima ya Mungu. 25 Kwa kuwa
ujinga wa Mungu una hekima kuliko ya wanadamu, na udhaifu wa Mungu una nguvu
zaidi ya wanadamu. 26 Angalia wito wa Mungu juu yenu, kaka na dada zangu. Si
wengi wenu mlikuwa na hekima katika viwango vya kibinadamu. Si wengi wenu
mlikuwa na nguvu. Si wengi wenu mlizaliwa katika ukuu. 27 Lakini Mungu alichagua
vitu vijinga vya dunia ili kuviaibisha vyenye hekima. Mungu alichagua kilicho
dhaifu katika dunia kukiaibisha chenye nguvu. 28 Mungu alichagua kile kilicho
cha hali ya chini na kilichodharauliwa katika dunia. Alichagua hata vitu ambavyo
havikuhesabiwa kuwa kitu, kwa kuvifanya si kitu vitu vilivyo na thamani. 29 Alifanya
hivi ili asiwepo yeyote aliye na sababu ya kujivuna mbele zake. 30 Kwa sababu ya kile
Mungu alichofanya, sasa mko ndani ya Kristo Yesu, ambaye amefanyika hekima kwa

ajili yetu kutoka kwa Mungu. Alikuwa haki yetu, utakatifu na ukombozi. 31 Kama
matokeo, kama andiko lisemavyo, "Anayejisifu, ajisifu katika Bwana."

# 2

1 Nilipokuja kwenu kaka na dada zangu, sikuja kwa maneno ya ushawishi na
hekima kama nilivyohubiri kweli iliyofichika kuhusu Mungu. 2 Niliamua kutojua
chochote nilipokuwa miongoni mwenu isipokuwa Yesu Kristo, na yeye aliyesulubiwa.
3 Na nilikuwa nanyi katika udhaifu, na katika hofu, na katika kutetemeka sana.
4 Na ujumbe wangu na kuhubiri kwangu hakukuwa katika maneno ya ushawishi
na hekima. Badala yake, yalikuwa katika kumdhihirisha Roho na ya nguvu, 5 ili
kwamba imani yenu isiwe katika hekima ya wanadadamu, bali katika nguvu ya
Mungu. 6 Sasa tunaizungumza hekima miongoni mwa watu wazima, lakini si hekima
ya dunia hii, au ya watawala wa nyakati hizi, ambao wanaopita. 7 Badala yake,
tunaizungumza hekima ya Mungu katika ukweli uliofichika, hekima iliyofichika
ambayo Mungu aliichagua kabla ya nyakati za utukufu wetu. 8 Hakuna yeyote wa
watawala wa nyakati hizi aliyeijua hekima hii, Kama wangeifahamu katika nyakati
zile, wasingelimsulubisha Bwana wa utukufu. 9 Lakini kama ilivyoandikwa, "Mambo
mbayo hakuna jicho limeyaona, hakuna sikio lililoyasikia, mawazo hayakufikiri,
mambo ambayo Mungu ameyaandaa kwa ajili ya wale wampendao yeye." 10 Haya
ni mambo ambayo Mungu ameyafunua kwetu kupitia Roho, Kwa kuwa Roho
huchunguza kila kitu, hata mambo ya ndani ya Mungu. 11 Kwa kuwa nani afahamuye
mawazo ya mtu, isipokuwa roho ya mtu ndani yake? Hivyo pia, hakuna ajuaye
mambo ya ndani ya Mungu, isipokuwa Roho wa Mungu. 12 Lakini hatukupokea
roho ya dunia, lakini Roho ambaye anatoka kwa Mungu, ili kwamba tuweze kujua
kwa uhuru mambo tuliyopewa na Mungu. 13 Tunasema mambo haya kwa maneno,
ambayo hekima ya mtu haiwezi kufundisha, lakini ambayo Roho hutufundisha. Roho
hutafasiri maneno ya kiroho kwa hekima ya kiroho. 14 Mtu asiye wa kiroho hapokei
mambo ambayo ni ya Roho wa Mungu, kwa kuwa hayo ni upuuzi kwake. Hawezi
kuyajua kwa sababu yanatambuliwa kiroho. 15 Kwa yule wa kiroho huhukumu
mambo yote. Lakini huhukumiwa na wengine. 16 "Ni nani anaweza kuyajua mawazo
ya Bwana, ambaye anaweza kumfundisha yeye?" Lakini tuna mawazo ya Kristo.

# 3

1 Na mimi, kaka na dada zangu, sikusema nanyi kama watu kiroho, lakini kama
na watu wa kimwili. Kama na watoto wadogo katika Kristo. 2 Niliwanywesha
maziwa na si nyama, kwa kuwa hamkuwa tayari kwa kula nyama. Na hata sasa
hamjawa tayari. 3 Kwa kuwa ninyi bado ni wa mwilini. Kwa kuwa wivu na majivuno
yanaonekana miongoni mwenu. Je, hamuishi kulingana na mwili, na je, hamtembei
kama kawaida ya kibinadamu? 4 Kwa kuwa mmoja husema, "Namfuata Paulo"
Mwingine husema "Namfuata Apolo," hamuishi kama wanadamu? 5 Apolo ni nani?
na Paulo ni nani? Watumishi wa yule mliyemwamini, kwa kila ambaye Bwana
alimpa jukumu. 6 Mimi nilipanda, Apolo akatia maji, lakini Mungu akakuza. 7 Kwa
hiyo, si aliye panda wala aliyetia maji ana chochote. Lakini ni Mungu anayekuza.
8 Sasa apandaye na atiaye maji wote ni sawa, na kila mmoja atapokea ujira wake
kulingana na kazi yake. 9 Kwa kuwa sisi tu watendakazi wa Mungu, ninyi ni bustani
ya Mungu, jengo la Mungu. 10 Kutokana na neema ya Mungu niliyopewa kama mjenzi
mkuu, niliuweka msingi, na mwingine anajenga juu yake. Lakini mtu awe makini
jinsi ajengavyo juu yake. 11 Kwa kuwa hakuna mwingine awezaye kujenga msingi
mwingine zaidi ya uliojengwa, ambao ni Yesu Kristo. 12 Sasa, kama mmoja wenu
ajenga juu yake kwa dhahabu, fedha, mawe ya thamani, miti, nyasi, au majani, 13 kazi

yake itafunuliwa, kwa mwanga wa mchana utaidhihirisha. Kwa kuwa itadhihirishwa
na moto. Moto utajaribu ubora wa kazi wa kila mmoja alichofanya. 14 Kama
chochote mtu alichojenga kitabaki, yeye atapokea zawadi. 15 Lakini kama kazi ya
mtu ikiteketea kwa moto, atapata hasara. Lakini yeye mwenyewe ataokolewa, kama
vile kuepuka katika moto. 16 Hamjui kuwa ninyi ni hekalu la Mungu na kwamba
Roho wa Mungu anakaa ndani yenu? 17 Kama mtu akiliharibu hekalu la Mungu,
Mungu atamharibu mtu yule. Kwa kuwa hekalu la Mungu ni takatifu, na hivyo na
ninyi. 18 Mtu asijidanganye mwenyewe, kama yeyote miongoni mwenu anadhani
ana hekima katika nyakati hizi, awe kama "mjinga" ndipo atakuwa na hekima.
19 Kwa kuwa hekima ya dunia hii ni ujinga mbele za Mungu, Kwa kuwa imeandikwa,
"Huwanasa wenye hekima kwa hila zao" 20 Na tena "Bwana anajua mawazo ya wenye
busara ni ubatili." 21 Hivyo mtu asijivunie wanadamu! Kwa kuwa vitu vyote ni vyenu.
22 Kama ni Paulo, au Apolo, au Kefa, au dunia, au maisha, au kifo, au vitu vilivyopo,
au vitakavyokuwepo. Vyote ni vyenu, 23 na ninyi ni wa Kristo na Kristo ni wa Mungu.

# 4

1 Hivi ndivyo mtu atuhesabu sisi, kama watumishi wa Kristo na mawakili wa siri
za kweli za Mungu. 2 Katika hili, kinachotakiwa kwa uwakili ni kwamba wawe wa
kutumainiwa. 3 Lakini kwangu mimi ni kitu kidogo sana kuwa ninahukumiwa na
ninyi au hukumu ya kibinadamu. Kwa kuwa sijihukumu hata mimi mwenyewe.
4 Sijihukumu mimi mwenyewe, hii haina maana kuwa mimi ni mwenye haki. Ni
Bwana anihukumuye. 5 Kwa hiyo, msitamke hukumu juu ya lolote kabla ya wakati,
kabla ya kuja kwa Bwana. Atayaleta nuruni mambo yaliyofichika gizani na kufunua
makusudi ya mioyo. Ndipo kila mmoja atapokea sifa yake kutoka kwa Mungu.
6 Sasa, kaka na dada zangu, mimi mwenyewe na Apolo nimetumia kanuni hizi
kwa ajili yenu. Ili kwamba kutoka kwetu mnaweza kujifunza maana ya usemi,
"Usiende zaidi ya kilivyoandikwa." Hii ni kwamba hakuna mmoja wenu ajivunaye
juu ya mwingine. 7 Maana ni nani aonaye tofauti kati yenu na mwingine? Ni
nini ulicho nacho hukukipokea bure? Kama umekwisha kupokea bure, kwa nini
mnajivuna kama hamkufanya hivyo? 8 Tayari mnavyo vyote ambavyo mngetaka!
Tayari mmekuwa na utajiri! Mmeanza kutawala-na kwamba mnamiliki zaidi yetu
sisi! Kweli, nawatakia umililki mwema ili kwamba tumiliki pamoja nanyi. 9 Kwa
hiyo ninadhani Mungu ametuweka sisi mitume kama kutuonyesha wa mwisho katika
mustari wa maandamano na kama watu waliohukumiwa kuuawa. Tumekuwa kama
tamasha kwa ulimwengu, kwa malaika na kwa wanadamu. 10 Sisi ni wajinga kwa
ajili ya Kristo, lakini ninyi ni wenye hekima katika Kristo. Tu wanyonge, lakini
ninyi mna nguvu. Mnaheshimiwa, lakina sisi tunadharauliwa. 11 Hata saa hii tuna
njaa na kiu, hatuna nguo, tuna mapigo, na tena hatuna makazi. 12 Tunafanya
kazi kwa bidii, kwa mikono yetu wenyewe. Tunapodharauliwa, twabariki. Wakati
tunapoteswa, twavumilia. 13 Tunapotukanwa, twarudisha kwa upole. Tumekuwa,
na tu bado tunahesabiwa kuwa kama kukataliwa na dunia na takataka kwa mambo
yote. 14 Siandiki mambo haya kuwaaibisha ninyi, lakini kuwarudi ninyi kama watoto
wangu niwapendao. 15 Hata kama mna waalimu makumi elfu katika Kristo, hamna
baba wengi. Kwa kuwa nimekuwa baba yenu katika Yesu Kristo kupitia injili.
16 Hivyo ninawasihi mniige mimi. 17 Hiyo ndiyo sababu nilimtuma kwenu Timotheo,
mpendwa wangu na mtoto mwaminifu katika Bwana. Atawakumbusheni njia zangu
katika Kristo, kama ninavyofundisha kila mahali na kila kanisa. 18 Sasa baadhi
yenu wanajisifu, wakitenda kana kwamba sitakuja kwenu. 19 Lakini nitakuja kwenu
kitambo, kama Bwana akipenda. Ndipo nitajua si maneno yao tu wanaojisifu, lakini
nitaona nguvu zao. 20 Kwa kuwa ufalme wa Mungu hauwi katika maneno bali katika

nguvu. [21] Mnataka nini? Nije kwenu na fimbo au kwa upendo na katika roho ya
upole?

# 5

[1] Tumesikia taarifa kuwa kuna zinaa miongoni mwenu, aina ya zinaa ambayo haipo
hata katikati ya watu wa Mataifa. Tuna taarifa kwamba mmoja wenu analala na
mke wa baba yake. [2] Nanyi mwajisifu! Badala ya kuhuzunika? Yule aliyefanya
hivyo anapaswa kuondolewa miongoni mwenu. [3] Ingawa sipo pamoja nanyi kimwili
lakini nipo nanyi kiroho, nimekwisha mhukumu yeye aliyefanya hivi, kama vile
nilikuwepo. [4] Mnapokutanika pamoja katika jina la Bwana wetu Yesu, na roho yangu
ipo pale kama kwa nguvu za Bwana wetu Yesu, nimekwisha mhukumu mtu huyu.
[5] Nimekwisha kumkabidhi mtu huyu kwa Shetani ili kwamba mwili wake uharibiwe,
ili roho yake iweze kuokolewa katika siku ya Bwana. [6] Majivuno yenu si kitu kizuri.
Hamjui chachu kidogo huharibu donge zima? [7] Jisafisheni ninyi wenyewe chachu ya
kale, ili kwamba muwe donge jipya, ili kwamba mwe mkate usiochachuliwa. Kwa
kuwa, Kristo, Mwana Kondoo wetu wa pasaka amekwisha kuchinjwa. [8] Kwa hiyo
tusherekee karamu si kwa chachu ya kale, chachu ya tabia mbaya na uovu. Badala
yake, tusherekee na mkate usiotiwa chachu wa unyenyekevu na kweli. [9] Niliandika
katika barua yangu kuwa msichangamane na wazinzi. [10] Sina maana wazinzi wa
dunia hii, au na wenye tamaa au wanyang'anyi au waabudu sanamu kwa kukaa mbali
nao, basi ingewapasa mtoke duniani. [11] Lakini sasa nawaandikia kutojichanganya na
yeyote anayeitwa kaka au dada katika Kristo, lakini anaishi katika uzinzi au ambaye
ni mwenye kutamani, au mnyang'anyi, au mwabudu sanamu, au mtukanaji au mlevi.
Wala msile naye mtu wa namna ile. [12] Kwa hiyo nitajihusishaje kuwahukumu walio
nje ya Kanisa? Badala yake, ninyi hamkuwahukumu walio ndani ya kanisa? [13] Lakini
Mungu anawahukumu walio nje. “Mwondoeni mtu mwovu miongoni mwenu”

# 6

[1] Mmoja wenu anapokuwa na tatizo na mwenzake, anathubutu kwenda kwa
mahakama ya wasio haki kuliko mbele ya waumini? [2] Hamjui kuwa waumini
watauhukumu ulimwengu? Na kama mtauhukumu ulimwengu, hamuwezi kuamua
mambo yasiyo muhimu? [3] Hamjui kuwa tutawahukumu malaika? Kwa kiasi gani
zaidi, tunaweza kuamua mambo ya maisha haya? [4] Kama tunaweza kuhukumu
mambo ya maisha haya, kwa nini mnathubutu kupeleka mashitaka mbele ya wasiosi-
mama kanisani? [5] Nasema haya kwa aibu yenu. Hakuna mwenye busara miongoni
mwenu wa kutosha kuweka mambo sawa kati ya ndugu na ndugu? [6] Lakini kama
ilivyo sasa, mwamini mmoja huenda mahakamani dhidi ya muumini mwingine, na
mashitaka hayo huwekwa mbele ya hakimu asiyeamini! [7] Ukweli ni kwamba kuna
matatizo katikati ya Wakristo yaliyoleta tayari usumbufu kwenu. Kwanini msiteseke
kwa mabaya? Kwanini mnakubali kudanganywa? [8] Lakini mmetenda uovu na
kudanganya wengine, na hao ni kaka na dada zenu! [9] Hamjui kwamba wasio haki
hawataurithi ufalme wa Mungu? Msiamini uongo. Waasherati, waabudu sanamu,
wazinzi, wafiraji, walawiti, [10] wevi, wachoyo, walevi, wanyang'anyi, watukanaji-
hakuna miongoni mwao atakayeurithi ufalme wa Mungu. [11] Na hao walikuwa
baadhi yao ni ninyi. Lakini mmekwisha kutakaswa, lakini mmekwisha kuoshwa,
lakini mmekwisha kutengwa kwa Mungu, lakini mmefanywa haki mbele za Mungu
katika jina la Bwana Yesu Kristo na kwa Roho wa Mungu wetu. [12] “Vitu vyote ni
halali kwangu”, lakini si kila kitu kina faida. “Vitu vyote ni halali kwangu,” lakini
sitatawaliwa na kimoja cha hivyo. [13] “Chakula ni kwa ajili ya tumbo, na tumbo ni
kwa ajili ya chakula,” lakini Mungu atavitowesha vyote. Mwili haujaumbwa kwa ajili

ya ukahaba, badala yake, mwili ni kwa ajili ya Bwana, na Bwana atauhudumia mwili.
14 Mungu alimfufua Bwana na sisi pia atatufufua kwa nguvu zake. 15 Hamjui kwamba
miili yenu ina muunganiko na Kristo? Mwawezaje kuvitoa viungo vya Kristo na
kwenda kuviunganisha na kahaba? Haiwezekani! 16 Hamjui kwamba anayeungana
na kahaba amekuwa mwili mmoja naye? Kama andiko lisemavyo, "Wawili watakuwa
mwili mmoja." 17 Lakini anayeungana na Bwana anakuwa roho moja pamoja naye.
18 Ikimbieni zinaa! "Kila dhambi aifanyayo mtu ni nje na mwili wake. Lakini zinaa,
mtu hutenda dhambi dhidi ya mwili wake mwenyewe. 19 Hamjui kuwa miili yenu
ni hekalu la Roho Mtakatifu, akaaye ndani yenu, yule ambaye mlipewa kutoka kwa
Mungu? Hamjui kwamba si ninyi wenyewe? 20 Kwamba mlinunuliwa kwa thamani.
Kwa hiyo mtukuzeni Mungu kwa miili yenu.

# 7

1 Kuhusu mambo mliyoniandikia: Kuna wakati ambapo ni vizuri mwanaume
asilale na mke wake. 2 Lakini kwa sababu ya majaribu mengi ya zinaa kila
mwanaume awe na mkewe, na kila mwanamke awe na mmewe. 3 Mume anapaswa
kumpa mke haki yake ya ndoa, na vile vile mke naye kwa mmewe. 4 Si mke aliye
na mamlaka juu ya mwili wake, ni mme. Na vile vile, mme naye hana mamlaka
juu ya mwili wake, bali mke anayo. 5 Msinyimane mnapolala pamoja, isipokuwa
mmekubaliana kwa muda maalum. Fanyeni hivyo ili kupata muda wa maombi.
Kisha mnaweza kurudiana tena pamoja, Ili kwamba Shetani asije akawajaribu kwa
kukosa kiasi. 6 Lakini nasema haya mambo kwa hiari na si kama amri. 7 Natamani
kila mmoja angekuwa kama mimi nilivyo. Lakini kila mmoja ana karama yake kutoka
kwa Mungu. Huyu ana karama hii, na yule ana karama ile. 8 Kwa wasioolewa
na wajane ninasema kwamba, ni vizuri kwao kama wakibaki bila kuolewa, kama
nilivyo mimi. 9 Lakini kama hawawezi kujizuia, wanapaswa kuolewa. Kwa kuwa
heri kwao kuolewa kuliko kuwaka tamaa. 10 Sasa kwa wale walioolewa nawapa
amri, si mimi bali ni Bwana. "Mke asitengane na mme wake." 11 Lakini kama
akijitenga kutoka kwa mmewe, abaki hivyo bila kuolewa au vinginevyo apatane na
mmewe. Na "Mme asimpe talaka mke wake." 12 Lakini kwa waliobaki, nasema-
mimi, si Bwana- kwamba kama ndugu yeyote ana mke asiyeamini na anaridhika
kuishi naye, hapaswi kumwacha. 13 Kama mwanamke ana mme asiyeamini, na
kama anaridhika kuishi naye, asimwache. 14 Kwa mme asiyeamini anatakaswa
kwa sababu ya imani ya mkewe. Na mwanamke asiyeamini anatakaswa kwa
sababu ya mmewe aaminiye. Vinginevyo watoto wenu wangekuwa si safi, lakini
kwa kweli wametakaswa. 15 Lakini mwenzi asiyeamini akiondoka na aende. Kwa
namna hiyo, kaka au dada hafungwi na viapo vyao. Mungu ametuita tuishi kwa
amani. 16 Unajuaje kama mwanamke, huenda utamwokoa mmeo? Au unajuaje kama
mwanaume, huenda utamwokoa mkeo? 17 Kila mmoja tu aishi maisha kama Bwana
alivyowagawia, kila mmoja kama Mungu alivyowaita wao. Huu ni mwongozo wangu
kwa makanisa yote. 18 Yupo aliyekuwa ametahiriwa alipoitwa kuamini? Asijaribu
kuondoa alama ya tohara yake. Yupo yeyote aliyeitwa katika imani hajatahiriwa?
Hapaswi kutahiriwa. 19 Kwa hili aidha ametahiriwa wala asiye tahiriwa hakuna
matatizo. Chenye matatizo ni kutii amri za Mungu. 20 Kila mmoja abaki katika
wito alivyokuwa alipoitwa na Mungu kuamini. 21 Ulikuwa mtumwa wakati Mungu
alipokuita? Usijali kuhusu hiyo. Lakini kama unaweza kuwa huru, fanya hivyo.
22 Kwa mmoja aliyeitwa na Bwana kama mtumwa ni mtu huru katika Bwana. Kama
vile, mmoja aliye huru alipoitwa kuamini ni mtumwa wa Kristo. 23 Mmekwisha
nunuliwa kwa thamani, hivyo msiwe watumwa wa wanadamu. 24 Kaka na dada
zangu, katika maisha yoyote kila mmoja wetu tulipoitwa kuamini, tubaki kama vile.

25 Sasa, wale wote ambao hawajaoa kamwe, sina amri kutoka kwa Bwana. Lakini
nawapa maoni yangu kama nilivyo. Kwa huruma za Bwana, zinazo aminika 26 Kwa
hiyo, ninafikiri hivyo kwa sababu ya usumbufu, ni vyema mwanaume abaki kama
alivyo. 27 Umefungwa kwa mwanamke na kiapo cha ndoa? Usitake uhuru kutoka kwa
hiyo. Una uhuru kutoka kwa mke au hujaolewa? Usitafute mke. 28 Lakini kama ukioa,
hujafanya dhambi. Na kama mwanamke hajolewa akiolewa, hajafanya dhambi. Bado
wale wanaoana wanapata masumbufu ya aina mbalimbali. Nami nataka niwaepushe
hayo. 29 Lakini nasema hivi, kaka na dada zangu, muda ni mfupi. Tangu sasa na
kuendelea, wale walio na wake waishi kama hawana. 30 Wote walio na huzuni
wajifanye kama walikuwa hawana huzuni, na wote wanaofurahi, kama walikuwa
hawafurahi, na wote wanaonunua kitu chochote, kama hawakumiliki chochote.
31 Na wote wanaoshughulika na ulimwengu, wawe kama hawakushughulika nao.
Kwa kuwa mitindo ya dunia inafikia mwisho wake. 32 Ninataka muwe huru kwa
masumbufu yote. Mwanaume asiyeoa anajihusisha na vitu vinavyo mhusu Bwana,
namna ya kumpendeza yeye. 33 Lakini mwanaume aliyeoa hujihusisha na mambo
ya dunia, namna ya kumpendeza mkewe, 34 amegawanyika. Mwanawake asiyeolewa
au bikira hujihusisha na vitu kuhusu Bwana, namna ya kujitenga katika mwili na
katika roho. Lakini mwanamke aliyeolewa hujihusisha kuhusu vitu dunia, namna ya
kumfurahisha mme wake. 35 Nasema hivi kwa faida yenu wenyewe, na siweki mtego
kwenu. Nasema hivi kwa vile ni haki, ili kwamba mnaweza kujiweka wakfu kwa
Bwana bila kikwazo chochote. 36 Lakini kama mtu anafikiri hawezi kumtendea kwa
heshima mwanawali wake, kwa sababu ya hisia zake zina nguvu sana, acha aoane
naye kama apendavyo. Siyo dhambi. 37 Lakini kama amefanya maamuzi kutokuoa,
na hakuna haja ya lazima, na kama anaweza kutawala hamu yake, atafanya vyema
kama hatamwoa. 38 Hivyo, anayemwoa mwanamwali wake afanya vyema, na yeyote
ambaye anachagua kutooa atafanya vyema zaidi. 39 Mwanamke amefungwa na
mmewe wakati yu hai. Lakini kama mmewe akifa, yuko huru kuolewa na yeyote
ampendaye, lakini katika Bwana tu. 40 Bado katika maamuzi yangu, atakuwa na
furaha zaidi kama akiishi kama alivyo. Na ninafikiri kuwa nami pia nina Roho wa
Mungu.

# 8

1 Sasa kuhusu vyakula vilivyotolewa sadaka kwa sanamu: tunajua ya kwamba
“sisi sote tuna maarifa.” Maarifa huleta majivuno, bali upendo hujenga. 2 Ikiwa mtu
yeyote anadhani kwamba anajua jambo fulani, mtu huyo bado hajui kama impasavyo
kujua. 3 Lakini ikiwa mmoja wapo akimpenda Mungu, mtu huyo anajulikana naye.
4 Basi kuhusu kula vyakula vilivyotolewa sadaka kwa sanamu: twajua kuwa “sanamu
si kitu katika dunia hii,” na ya kuwa hakuna Mungu ila mmoja tu.” 5 Kwa maana
kuna wengi waitwao miungu ikiwa ni mbinguni au duniani, kama vile walivyo
“miungu na mabwana wengi.” 6 “Ijapokuwa kwetu kuna Mungu mmoja tu ambaye
ni Baba, vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake, na Bwana mmoja Yesu
Kristo, ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo, na kwa yeye sisi tupo.” 7 Hata hivyo,
ujuzi huu haupo ndani ya kila mmoja. Badala yake, wengine walishiriki ibada za
sanamu hapo zamani, na hata sasa wanakula vyakula hivi kana kwamba ni kitu
kilichotolewa sadaka kwa sanamu. Dhamiri zao zimepotoshwa kwa kuwa ni dhaifu.
8 Lakini chakula hakitatuthibitisha sisi kwa Mungu. Sisi sio wabaya sana kama
tusipo kula, wala wema sana ikiwa tutakula. 9 Lakini iweni makini ya kwamba
uhuru wenu usiwe sababu ya kumkwaza aliye dhaifu katika imani. 10 Hebu fikiri
kwamba mtu amekuona, wewe uliye na ujuzi, unakula chakula katika hekalu la
sanamu. Dhamiri yake mtu huyo haitathibitika hata yeye naye ale vitu vilivyotolewa

sadaka kwa sanamu? [11] Kwa hiyo kwa sababu ya ufahamu wako wa ukweli juu ya
asili ya sanamu, kaka au dada yako aliye dhaifu, ambaye pia Kristo alikufa kwa ajili
yake, anaangamizwa. [12] Hivyo, unapofanya dhambi dhidi ya kaka na dada zako na
kuzijeruhi dhamiri zao zilizo dhaifu, mnatenda dhambi dhidi ya Kristo. [13] Kwa hiyo,
ikiwa chakula kinasababisha kumkwaza kaka au dada, sitakula nyama kamwe, ili
nisimsababishe kaka au dada yangu kuanguka.

# 9

[1] Mimi si huru? Mimi si mtume? Mimi sikumwona Yesu Bwana wetu? Ninyi
si matunda ya kazi yangu katika Bwana? [2] Ikiwa mimi si mtume kwa wengine,
angalau ni mtume kwenu ninyi. Kwa maana ninyi ni uthibitisho wa utume wangu
katika Bwana. [3] Huu ndio utetezi wangu kwa wale wanaonichunguza mimi. [4] Je
hatuna haki ya kula na kunywa? [5] Hatuna haki kuchukua mke aliye amini kama
wafanyavyo mitume wengine, na ndugu wa Bwana, na Kefa? [6] Au ni mimi peke yangu
na Barnaba ambao tunapaswa kufanya kazi? [7] Ni nani afanyaye kazi kama askari
kwa gharama zake mwenyewe? Ni nani apandaye mzabibu na asile matunda yake?
Au ni nani achungaye kundi asiyekunywa maziwa yake? [8] Je ninasema haya kwa
mamlaka ya kibinadamu? Sheria nayo haisemi haya? [9] Kwa kuwa imeandikwa katika
sheria ya Musa, "usimfunge ng'ombe kinywa apulapo nafaka." Ni kweli kwamba
hapa Mungu anajali ng'ombe? [10] Au je hasemi hayo kwa ajili yetu? imeandikwa
kwa ajili yetu, kwa sababu yeye alimaye nafaka inampasa kulima kwa matumaini,
naye avunaye inampasa avune kwa matarajio ya kushiriki katika mavuno. [11] Ikiwa
tulipanda vitu vya rohoni miongoni mwenu, Je! Ni neno kubwa kwetu tukivuna vitu
vya mwilini kutoka kwenu? [12] Ikiwa wengine walipata haki hii kutoka kwenu, Je!
Sisi si zaidi? Hata hivyo, hatukuidai haki hii. Badala yake, tulivumilia mambo yote
badala ya kuwa kikwazo cha injili ya Kristo. [13] Hamjui ya kuwa wote wafanyao kazi
hekaluni hupata chakula chao kutoka hekaluni? Hamjui ya kuwa wote watendao
kazi madhabahuni hupata sehemu ya kile kilichotolewa madhabahuni? [14] Kwa jinsi
iyo hiyo, Bwana aliagiza ya kuwa wote wanaoitangaza injili sharti wapate kuishi
kutokana na hiyo injili. [15] Lakini sijawadai haki zote hizi. Na siandiki haya ili jambo
lolote lifanyike kwa ajili yangu. Ni heri mimi nife kuliko mtu yeyote kubatilisha huku
kujisifu kwangu. [16] Maana ikiwa naihubiri injili, sina sababu ya kujisifu, kwa sababu
ni lazima nifanye hivi. Na ole wangu nisipoihubiri injili! [17] Kwa maana nikifanya
hivi kwa hiari yangu, nina thawabu. Lakini ikiwa si kwa hiari, bado nina jukumu
nililopewa kuwa wakili. [18] Basi thawabu yangu ni nini? Ya kuwa nihubiripo, nitaitoa
injili pasipo gharama na bila kutumia kwa utimilifu wa haki yangu niliyonayo katika
Injili. [19] Maana japo nimekuwa huru kwa wote, nilifanyika mtumwa wa wote, ili
kwamba niweze kuwapata wengi zaidi. [20] Kwa Wayahudi nilikuwa kama Myahudi,
ili niwapate Wayahudi. Kwa wale walio chini ya sheria, nilikuwa kama mmoja wao
aliye chini ya sheria ili niwapate wale walio chini ya sheria. Nilifanya hivyo ingawa
mimi binafsi sikuwa chini ya sheria. [21] Kwa wale walio nje ya sheria, nilikuwa kama
mmoja wao nje ya sheria, ingawa mimi binafsi sikuwa nje ya sheria ya Mungu, bali
chini ya sheria ya Kristo. Nilifanya hivyo ili niwapate wale walio nje ya sheria. [22] Kwa
walio wanyonge nilikuwa mnyonge, ili niwapate walio wanyonge. Nimekuwa hali
zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa baadhi. [23] Nami nafanya
mambo yote kwa ajili ya injili, ili nipate kushiriki katika baraka. [24] Hamjui ya kuwa
katika mbio wote washindanao hupiga mbio, lakini apokeaye tuzo ni mmoja? Hivyo
pigeni mbio ili mpate tuzo. [25] Mwana michezo hujizuia katika yote awapo katika
mafunzo. Hao hufanya hivyo ili wapokee taji iharibikayo, lakini sisi tunakimbia ili
tupate taji isiyoharibika. [26] Kwa hiyo mimi sikimbii bila sababu au napigana ngumi

kama kupiga hewa. 27 Lakini nautesa mwili wangu na kuufanya kama mtumwa, ili
kwamba nijapokwisha kuwahubiri wengine, mimi mwenyewe nisiwe wa kukataliwa.

# 10

1 Nataka ninyi mjue kaka na dada zangu, ya kuwa baba zetu walikuwa chini
ya wingu na wote walipita katika bahari. 2 Wote walibatizwa wawe wa Musa
ndani ya wingu na ndani ya bahari, 3 na wote walikula chakula kile kile cha
roho. 4 Wote walikunywa kinywaji kile kile cha roho. Maana walikunywa kutoka
katika mwamba wa roho uliowafuata, na mwamba ule ulikuwa ni Kristo. 5 Lakini
Mungu hakupendezwa sana na wengi wao, na maiti zao zilisambazwa jangwani.
6 Basi mambo haya yote yalikuwa mifano kwetu, ili sisi tusiwe watu wa kutamani
mabaya kama na wao walivyofanya. 7 Msiwe waabudu sanamu, kama wengine
wao walivyokuwa. Hii ni kama ilivyoandikwa, "Watu walikaa chini wakila na
kunywa, na waliinuka kucheza kwa tamaa za mapenzi." 8 Tusifanye uasherati kama
wengi wao walivyofanya. Wakafa siku moja watu ishirini na tatu elfu kwa sababu
hiyo. 9 Wala tusimjaribu Kristo, kama wengi wao walivyofanya na wakaharibiwa
kwa nyoka. 10 Na pia msinung'unike, kama wengi wao walivyonung'unika na
kuharibiwa na malaika wa mauti. 11 Basi mambo hayo yalitendeka kama mifano
kwetu. Yakaandikwa ili kutuonya sisi - tuliofikiliwa na miisho ya zamani. 12 Kwa hiyo
kila ajionaye amesimama awe makini asije akaanguka. 13 Hakuna jaribu lililowapata
ninyi lisilo kawaida ya wanadamu. Ila Mungu ni mwaminifu. Hatawaacha mjaribiwe
kupita uwezo wenu. Pamoja na jaribu yeye atawapa mlango wa kutokea, ili mweze
kustahimili. 14 Kwa hiyo, wapendwa wangu, ikimbieni ibada ya sanamu. 15 Nasema
nanyi kama watu wenye akili, ili muamue juu ya ninalosema. 16 Kikombe cha baraka
tubarikicho, si ushirika wa damu ya Kristo? Mkate ule tuumegao, si ushirika wa
mwili wa Kristo? 17 Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja.
Sisi sote twapokea mkate mmoja kwa pamoja. 18 Watazameni watu wa Israeli: Je!
Wale wote walao dhabihu si washiriki katika madhabahu? 19 Nasema nini basi?
Ya kuwa sanamu ni kitu? Au ya kuwa chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu
ni kitu? 20 Lakini nasema juu ya vitu vile wavitoavyo sadaka watu wapagani wa
Mataifa, ya kuwa wanatoa vitu hivi kwa mapepo na sio kwa Mungu. Nami sitaki
ninyi kushirikiana na mapepo! 21 Hamwezi kunywea kikombe cha Bwana na kikombe
cha mapepo. Hamwezi kuwa na ushirika katika meza ya Bwana na katika meza ya
mapepo. 22 Au twamtia Bwana wivu? Tuna nguvu zaidi yake? 23 "Vitu vyote ni
halali," lakini si vyote vifaavyo. "Vitu vyote ni halali," lakini si vyote viwajengavyo
watu. 24 Hakuna hata mmoja angetafuta mazuri yake tu. Badala yake, kila mmoja
angetafuta mazuri ya mwenzake. 25 Mnaweza kula kila kitu kiuzwacho sokoni bila
kuuliza -uliza kwa ajili ya dhamiri. 26 Maana "dunia ni mali ya Bwana, na vyote
viijazavyo." 27 Na mtu asiyeamini akiwaalika kula, na mnataka kwenda, kuleni
chochote awapacho pasipo kuuliza maswali ya dhamiri. 28 Lakini mtu akiwaambia,
"Chakula hiki kimetokana na sadaka ya wapagani," msile. Hii ni kwa ajili yake
aliyewaambia, na kwa ajili ya dhamiri. 29 Nami simaanishi dhamiri zenu, bali
dhamiri ya yule mwingine. Maana kwanini uhuru wangu uhukumiwe na dhamiri ya
mtu mwingine? 30 Ikiwa mimi natumia chakula kwa shukrani, kwanini nitukanwe
kwa kitu ambacho nimeshukuru kwacho? 31 Kwa hiyo, chochote mnachokula au
kunywa, au chochote mfanyacho, fanyeni yote kwa ajili ya utukufu wa Mungu.
32 Msiwakoseshe Wayahudi au Wayunani, au kanisa la Mungu. 33 Jaribuni kama
mimi ninavyojaribu kuwapendeza watu wote kwa mambo yote. Sitafuti faida yangu
mwenyewe, bali ya wengi. Nami nafanya hivi ili wapate kuokolewa.

# 11

1 Nifuateni mimi, kama na mimi ninavyomfuata Kristo. 2 Sasa nawasifu kwasababu
ya vile mnavyonikumbuka katika mambo yote. Nawasifu kwasababu mmeyashika
mapokeo kama nilivyoyaleta kwenu. 3 Basi nataka mfahamu ya kuwa Kristo ni
kichwa cha kila mwanaume, naye mwanaume ni kichwa cha mwanamke, na ya kuwa
Mungu ni kichwa cha Kristo. 4 Kila mwanaume aombaye au atoae unabii akiwa
amefunika kichwa anakiabisha kichwa chake. 5 Lakini kila mwanamke aombae
au kutoa unabii hali kichwa chake kikiwa wazi anakiaibisha kichwa chake. Kwa
maana ni sawa sawa na kama amenyolewa. 6 Ikiwa kama mwanamke hatafunika
kichwa chake, na akatwe nywele zake ziwe fupi. Maana ikiwa ni aibu mwanamke
kukata nywele zake au kunyolewa, basi afunike kichwa chake. 7 Kwani haimpasi
mwanamume kufunika kichwa chake, kwa sababu yeye ni mfano na utukufu wa
Mungu. Lakini mwanamke ni utukufu wa mwanamume. 8 Maana mwanamume
hakutokana na mwanamke. Bali mwanamke alitokana na mwanamume. 9 Wala
mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke. Bali mwanamke aliumbwa
kwa ajili ya mwanamume. 10 Hii ndio sababu mwanamke anapaswa kuwa na
ishara ya mamlaka juu ya kichwa chake, kwa sababu ya malaika. 11 Hata hivyo,
katika Bwana, mwanamke hayupo peke yake pasipo mwanamume, au mwanamume
pasipo mwanamke. 12 Maana kama vile mwanamke alitoka kwa mwanamume,
vile vile mwanamume alitoka kwa mwanamke. Na vitu vyote hutoka kwa Mungu.
13 Hukumuni wenyewe: Je! ni sahihi mwanamke amuombe Mungu hali kichwa chake
kikiwa wazi? 14 Je hata asili peke yake haiwafundishi ya kwamba mwanamume akiwa
na nywele ndefu ni aibu kwake? 15 Je asili haiwafundishi ya kwamba mwanamke
akiwa na nywele ndefu ni utukufu kwake? Maana amepewa zile nywele ndefu kama
vazi lake. 16 Lakini ikiwa mtu yeyote anataka kubishana juu ya hili, sisi hatuna
namna nyingine, wala makanisa ya Mungu. 17 Katika maagizo yafuatayo, mimi
siwasifu. Maana mnapokusanyika, sio kwa faida bali kwa hasara. 18 Maana kwanza,
nasikia ya kuwa mkutanikapo kanisani, kuna migawanyiko kati yenu, na kwa sehemu
ninaamini. 19 Kwa maana ni lazima iwepo misuguano kati yenu, ili kwamba wale
waliokubaliwa wajulikane kwenu. 20 Kwa maana mkutanikapo, mnachokula sio
chakula cha Bwana. 21 Mnapokula, kila mmoja hula chakula chake mwenyewe
kabla wengine hawajala. hata huyu ana njaa, na huyu amelewa. 22 Je hamna
nyumba za kulia na kunywea? Je mnalidharau kanisa la Mungu na kuwafedhehesha
wasio na Kitu? Niseme nini kwenu? Niwasifu? Sitawasifu katika hili! 23 Maana
nilipokea kutoka kwa Bwana kile ambacho nimewapa ninyi ya kuwa Bwana Yesu,
usiku ule aliposalitiwa, alichukua mkate. 24 Baada ya kushukuru, aliuvunja na
kusema, “Huu ndio mwili wangu, ulio kwa ajili yenu. Fanyeni hivi kwa kunikumbuka
mimi.” 25 Na vivi hivi akachukua kikombe baada ya kula, na kusema, “Kikombe
hiki ni agano jipya katika damu yangu. Fanyeni hivi mara nyingi kila mywapo, kwa
kunikumbuka mimi.” 26 Kwa kila muda mlapo mkate huu na kukinywea kikombe,
mwaitangaza mauti ya Bwana mpaka atakapokuja. 27 Kwa hiyo, kila aulaye mkate
au kukinywea kikombe hicho cha Bwana isivyostahili, atakuwa amejipatia hatia
ya mwili na damu ya Bwana. 28 Mtu ajihoji mwenyewe kwanza, na hivyo aule
mkate, na kukinywea kikombe. 29 Maana alaye na kunywa bila kuupambanua mwili,
hula na kunywa hukumu yake mwenyewe. 30 Hii ndiyo sababu watu wengi kati
yenu ni wagonjwa na dhaifu, na baadhi yenu wamekufa. 31 Lakini tukijichunguza
wenyewe hatutahukumiwa. 32 Ila tunapohukumiwa na Bwana, twarudiwa, ili tusije
tukahukumiwa pamoja na dunia. 33 Kwa hiyo, kaka na dada zangu, mkutanikapo
mpate kula, ngojeaneni. 34 Mtu akiwa na njaa, na ale nyumbani kwake, ili kwamba
mkutanikapo pamoja isiwe kwa hukumu. Na kuhusu mambo mengine mliyoandika,

nitawaelekeza nitakapokuja.

# 12

1 Kuhusu karama za rohoni, kaka na dada zangu sitaki mkose kufahamu. 2 Mwajua
ya kuwa mlipokuwa wapagani mliongozwa kufuata sanamu zisizoongea, kwa njia
zozote mliongozwa nazo. 3 Kwa hiyo, nataka mfahamu kwamba hakuna yeyote
anenaye kwa Roho wa Mungu akisema, “Yesu amelaaniwa.” Hakuna yeyote
atakayesema, “Yesu ni Bwana,” isipokuwa katika Roho Mtakatifu. 4 Basi kuna karama
tofauti tofauti, bali Roho ni yeye yule. 5 Na kuna huduma tofauti tofauti, bali Bwana ni
yeye yule. 6 Na kuna aina mbalimbali za kazi, lakini Mungu ni yeye yule azitendaye
kazi zote katika wote. 7 Basi kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa faida ya
wote. 8 Maana mtu mmoja amepewa na Roho neno la hekima, na mwingine neno
la maarifa kwa Roho yule yule. 9 Kwa mwingine humpa imani kwa Roho yeye yule,
na kwa mwingine karama ya uponyaji kwa Roho mmoja. 10 Kwa mwingine matendo
ya nguvu, na mwingine unabii. Na kwa mwingine uwezo wa kupambanua roho,
mwingine aina mbalimbali za lugha, na kwa mwingnine tafsiri za lugha. 11 Lakini
Roho ni yule yule atendaye kazi hizi zote, kumpa kila mtu karama kwa kadiri ya
uchaguzi wake mwenyewe. 12 Kwa maana kama vile mwili ni mmoja, nao una
viungo vingi, na viungo vyote ni vya mwili ule ule, vivyo hivyo na Kristo. 13 Kwa
maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu
Wayahudi au Wayunani, kwamba tu watumwa au huru, na wote tulinyweshwa
Roho mmoja. 14 Kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali ni vingi. 15 Ikiwa mguu
utasema, “kwa kuwa mimi si mkono, mimi si sehemu ya mwili,” hiyo haiufanyi
kutokuwa sehemu ya mwili. 16 Na ikiwa sikio litasema, “kwa kuwa mimi si jicho,
mimi si sehemu ya mwili,” hiyo hailifanyi kutokuwa sehemu ya mwili. 17 Kama
mwili wote utakuwa jicho, kungekuwa wapi kusikia? Kama mwili wote ukiwa sikio,
kungekuwa wapi kunusa? 18 Lakini Mungu aliweka kila kiungo cha mwili mahali
pake kama alivyopanga mwenyewe. 19 Na kama vyote vingekuwa kiungo kimoja,
mwili ungekuwa wapi? 20 Hivyo sasa viungo ni vingi, lakini mwili ni mmoja. 21 Jicho
haliwezi kuuambia mkono, “sina haja na wewe.” Wala kichwa hakiwezi kuiambia
miguu, sina haja na ninyi.” 22 Lakini viungo vya mwili vinavyoonekana kuwa na
heshima kidogo vyahitajika zaidi. 23 Na viungo vya mwili tunavyodhani vina heshima
kidogo, twavipa heshima zaidi, na viungo vyetu visivyo na mvuto vina uzuri zaidi.
24 Na sasa viungo vyetu vilivyo na mvuto havina haja ya kupewa heshima, kwa
kuwa tayari vina heshima. Lakini Mungu ameviunganisha viungo vyote pamoja,
na amevipa heshima zaidi vile visivyo heshimiwa. 25 Alifanya hivyo ili pasiwepo
mgawanyiko katika mwili, bali viungo vyote vitunzane kwa upendo wa mmoja. 26 Na
wakati kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote vyaumia kwa pamoja. Au wakati kiungo
kimoja kikiheshimiwa, viungo vyote vifurahi kwa pamoja. 27 Sasa ninyi ni mwili
wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake. 28 Na Mungu ameweka katika kanisa
kwanza mitume, pili manabii, tatu waalimu, kisha wale wote watendao matendo
makuu, kisha karama za uponyaji, wale wasaidiao, wale wafanyao kazi ya kuongoza,
na wote walio na aina mbalimbali za lugha. 29 Je sisi sote ni mitume? Sisi sote ni
manabii? Sisi sote ni waalimu? Je sisi sote tunafanya matendo ya miujiza? 30 Je sisi
sote tuna karama ya uponyaji? Sisi sote tunaongea kwa lugha? Sisi sote tunatafsiri
lugha? 31 Tafuteni sana karama zilizo kuu. Nami nitawaonesha njia iliyo bora zaidi.

# 13

1 Tuseme kwamba ninanena kwa lugha za wanadamu na za malaika. Lakini kama
sina upendo, nimekuwa shaba iliayo au upatu uvumao. 2 Na kwamba nina karama

ya unabii na ufahamu wa kweli zilizofichika na maarifa, na kwamba ninayo imani
ya kuhamisha milima. Lakini ikiwa sina upendo, mimi si kitu. 3 Na tuseme kwamba
ninatoa milki yangu yote na kuwalisha masikini, na kwamba ninautoa mwili wangu
ili nichomwe moto. Lakini kama sina upendo, hainifaidii kitu. 4 Upendo huvumilia
na hufadhili. Upendo haujisifu au kujivuna. Hauna kiburi 5 au ukorofi. Hautafuti
mambo yake, hauoni uchungu haraka, wala hauhesabu mabaya. 6 Haufurahii
udhalimu. Badala yake, hufurahi katika kweli. 7 Upendo huvumilia mambo yote;
huamini mambo yote, una ujasiri katika mambo yote, na hustahimili mambo yote.
8 Upendo haukomi. Ikiwa kuna unabii, wote utapita. Ikiwa kuna lugha, zitakoma.
Ikiwa kuna maarifa, yatapita. 9 Kwa kuwa tunajua kwa sehemu na tunafanya unabii
kwa sehemu. 10 Lakini ijapo ile iliyo kamili, ile isiyo kamili itapita. 11 Nilipokuwa
mtoto, nilisema kama mtoto, nilifikiri kama mtoto, niliamua kama mtoto. Nilipokuwa
mtu mzima, niliweka mbali nami mambo ya kitoto. 12 Kwa kuwa sasa tunaona kama
kwa kioo, kama sura gizani, lakini wakati ule tutaona uso kwa uso. Sasa ninajua kwa
sehemu, lakini wakati ule nitajua sana kama na mimi ninavyojulikana sana. 13 Lakini
sasa mambo haya matatu yanadumu: imani, tumaini lijalo, na upendo. Lakini lililo
kuu zaidi ya haya ni upendo.

# 14

1 Utafuteni upendo na kutamani sana karama za rohoni, zaidi sana mpate kutoa
unabii. 2 Maana yeye anenaye kwa lugha hasemi na watu bali husema na Mungu.
Maana hakuna aelewaye kwa sababu anena mambo yaliyofichika katika Roho.
3 Lakini yeye atoaye unabii, asema na watu na kuwajenga, kuwatia moyo, na
kuwafariji. 4 Yeye anenaye kwa lugha hujijenga mwenyewe, lakini yeye atoaye
unabii hulijenga kanisa. 5 Sasa natamani kwamba ninyi nyote mnene kwa lugha.
Lakini zaidi ya hayo, natamani ya kwamba mtoe unabii. Yeye atoaye unabii ni mkuu
kuliko yeye anenaye kwa lugha (labda awepo wa kutafasiri), ili kwamba kanisa lipate
kujengwa. 6 Lakini sasa, kaka na dada zangu, nikija kwenu na kunena kwa lugha,
nitawafaidia nini ninyi? Siwezi, isipokuwa nasema nanyi kwa njia ya ufunuo, au
kwa njia ya maarifa, au unabii, au kwa njia ya fundisho. 7 Ikiwa vitu visivyo na uhai
kama filimbi au kinubi visipotoa sauti zilizo na tofauti, itatambulikanaje ni chombo
gani kinachezwa? 8 Kwa maana ikiwa baragumu itatoa sauti isiyojulikana, ni jinsi
gani mtu atatambua ya kuwa ni muda wa kujiandaa kwa vita? 9 Vivyo hivyo na
ninyi. Mkitoa kwa ulimi neno lisilo dhahiri, ni jinsi gani mtu ataelewa mnachosema?
Mtakuwa mkiongea, na hakuna atakayewaelewa. 10 Hakuna shaka kwamba kuna
lugha nyingi mbalimbali duniani, na hakuna hata moja isiyo na maana. 11 Lakini
ikiwa sijui maana ya lugha, nitakuwa mgeni kwake yeye anenaye, naye anenaye
atakuwa mgeni kwangu. 12 Vivyo hivyo na ninyi. Kwa kuwa mnatamani sana kuona
uthihirisho wa Roho, takeni kwamba mzidi sana kulijenga kanisa. 13 Hivyo, yeye
anenaye kwa lugha na aombe apewe kutafasiri. 14 Kwa maana nikiomba kwa lugha,
roho yangu huomba, lakini akili zangu hazina matunda. 15 Nifanye nini? Nitaomba
kwa roho yangu, lakini pia nitaomba kwa akili zangu. Nitaimba kwa roho yangu,
na nitaimba kwa akili zangu pia. 16 Vinginevyo, ukimsifu Mungu kwa roho, yeye
aliye mgeni ataitikaje "Amina" utoapo shukurani, akiwa hayajui usemayo? 17 Maana
ni kweli wewe washukuru vema, lakini yule mwingine hajengwi. 18 Namshukuru
Mungu kwa kuwa nanena kwa lugha zaidi ya ninyi nyote. 19 Lakini katika kanisa ni
heri ninene maneno matano kwa ufahamu wangu ili nipate kuwafundisha wengine,
zaidi ya kunena maneno kumi elfu kwa lugha. 20 Kaka na dada zangu, msiwe
watoto katika kufikiri kwenu. Badala yake, kuhusiana na uovu, iweni kama watoto
wachanga. Lakini katika kufikiri kwenu mkawe watu wazima. 21 Imeandikwa katika

sheria, “Kwa watu wa lugha nyingine na kwa midomo ya wageni nitasema na watu
hawa. Wala hata hivyo hawatanisikia,” asema Bwana. 22 Hivyo, ndimi ni ishara,
sio kwa walioamini, bali kwa wasioamini. Lakini kutoa unabii ni ishara, sio kwa
wasioamini, bali kwa ajili yao waaminio. 23 Haya, ikiwa kanisa lote limekusanyika
pamoja na wote wanene kwa lugha, na wageni na wasioamini wameingia, je
hawawezi kusema kwamba mna wazimu? 24 Lakini ikiwa wote mnatoa unabii na
asiyeamini au mgeni akaingia, atashawishiwa na yote asikiayo. Atahukumiwa na
yote yasemwayo. 25 Siri za moyo wake zingefunuliwa. Matokeo yake, angeanguka
kifudifudi na kumwabudu Mungu. Angekiri ya kwamba Mungu yu kati yenu. 26 Nini
kifuatacho basi, kaka na dada zangu? Mnapokutana pamoja, kila mmoja ana Zaburi,
mafundisho, mafunuo, lugha au tafsiri. Fanyeni kila kitu ili kwamba mlijenge kanisa.
27 Kama yeyote ananena kwa lugha, wawepo wawili au watatu, na kila mmoja
katika zamu. Na mtu lazima atafasiri kilichosemwa. 28 Lakini kama hakuna mtu
wa kutafasiri, basi kila mmoja wao akae kimya ndani ya kanisa. Basi kila mmoja
aongee peke yake na kwa Mungu. 29 Na manabii wawili au watatu wanene, na
wengine wasikilize kwa kupambanua kilichosemwa. 30 Lakini aliyeketi akifunuliwa
jambo katika huduma, yule ambaye alikuwa ananena na anyamaze. 31 Kwa kuwa
kila mmoja wenu anaweza kutoa unabii mmoja baada ya mwingine ili kwamba kila
mmoja aweze kujifunza na wote waweze kutiwa moyo. 32 Kwa kuwa roho za manabii
ziko chini ya uangalizi wa manabii. 33 Kwa kuwa Mungu si Mungu wa machafuko, bali
wa amani. Kama ilivyo katika makanisa yote ya waumini, 34 imewapasa wanawake
wakae kimya katika kanisa. Kwa kuwa hawaruhusiwi kuzungumza. Badala yake,
wanapaswa kuwa katika unyenyekevu, kama pia sheria inavyosema. 35 Kama kuna
chochote wanatamani kujifunza, basi wawaulize waume zao nyumbani. Kwa kuwa
ni aibu kwa mwanamke kuongea katika kanisa. 36 Je neno la Mungu lilitoka kwenu?
Je limewafikia ninyi tu? 37 Kama mtu akijiona kuwa ni nabii au wa rohoni, inampasa
ayatambue mambo ninayowaandikia ya kwamba ni maagizo ya Bwana. 38 Lakini
asipotambua haya, mwacheni asitambuliwe. 39 Hivyo basi, kaka na dada zangu,
takeni sana kutoa unabii, na msimzuie mtu yeyote kunena kwa lugha. 40 Lakini
mambo yote yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu.

# 15

1 Sasa ninawakumbusha, akina kaka na akina dada, juu ya injili niliyowahubiria,
ambayo mliipokea na kusimama kwayo. 2 Ni katika injili hii mmeokolewa, kama
mkilishika imara neno nililowahubiri ninyi, isipokuwa mliamini bure. 3 Kama
kwanza nilivyo ipokea kwa umuhimu niliileta kwenu kama ilivyo: kwamba kutokana
na maandiko, Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, 4 kutokana na maandiko
alizikwa, na kwamba alifufuka siku ya tatu. 5 Na kwamba alimtokea Kefa, kisha kwa
wale kumi na wawili. 6 Kisha aliwatokea kwa wakati mmoja akina kaka na akina
dada zaidi ya mia tano. Wengi wao bado wako hai, lakini baadhi yao wamelala
usingizi. 7 Kisha alimtokea Yakobo, kisha mitume wote. 8 Mwisho wa yote, alinitokea
mimi, kama vile kwa mtoto aliye zaliwa katika wakati usio sahihi. 9 Kwa kuwa mimi
ni mdogo kati ya mitume. Sistahili kuitwa mtume, kwa sababu nililitesa kanisa
la Mungu. 10 Lakini kwa neema ya Mungu nipo kama nilivyo, na neema yake
kwangu haikuwa bure. Badala yake, nilifanya bidii kuliko wote. Lakini haikuwa
mimi, bali neema ya Mungu iliyo ndani yangu. 11 Kwa hiyo kama ni mimi au
wao, tuna hubiri hivyo na tunaamini hivyo. 12 Sasa kama Kristo alihubiriwa kama
aliyefufuka kwa wafu, iweje baadhi yenu mseme hakuna ufufuo wa wafu? 13 Lakini
kama hakuna ufufuo wa wafu, basi hata Kristo pia hakufufuka. 14 Na kama Kristo
hakufufuka, hivyo mahubiri yetu ni bure, na imani yenu ni bure. 15 Na tumepatikana

kuwa mashahidi wa uongo kumuhusu Mungu, kwa sababu tulimshushuhudia Mungu
kinyume, kusema alimfufua Kristo, wakati hakumfufua. 16 Kama ikiwa wafu
hawafufuliwi, Yesu pia hakufufuliwa. 17 Na kama Kristo hakufufuliwa, imani yenu ni
bure na bado mko kwenye dhambi zenu. 18 Hivyo hata wale waliokufa katika Kristo
pia wameangamia. 19 Ikiwa kwa maisha haya peke yake tunaujasiri kwa wakati ujao
ndani ya Kristo, watu wote, sisi niwakuhurumiwa zaidi ya watu wote. 20 Lakini
sasa Kristo amefufuka kutoka kwa wafu, matunda ya kwanza ya wale waliokufa.
21 Kwa kuwa kifo kilikuja kupitia mwanadamu, pia kupitia mwanadamu ufufuo wa
wafu. 22 Kwa kuwa kama katika Adam wote wanakufa, hivyo pia katika Kristo
wote watafanywa hai. 23 Lakini kila moja katika mpango wake: Kristo, matunda
ya kwanza, na kisha wale walio wa Kristo watafanywa hai wakati wa kuja kwake.
24 Ndipo utakuwa mwisho, pale Kristo atakapo kabidhi ufalme kwa Mungu Baba. Hii
ni pale atakapo komesha utawala wote na mamlaka yote na nguvu. 25 Kwa kuwa
lazima atawale mpaka atakapoweka maadui zake wote chini ya nyayo zake. 26 Adui
wa mwisho kuharibiwa ni kifo. 27 Kwa kuwa “ameweka kila kitu chini ya nyayo
zake.” Lakini inaposema “ameweka kila kitu,” ni wazi kwamba hii haihusishi wale
walioweka kila kitu chini yake mwenyewe. 28 Wakati vitu vyote vimewekwa chini
yake, kisha Mwana mwenyewe atawekwa chini kwake Yeye ambaye aliviweka vitu
vyote chini yake. Hii itatokea ili kwamba Mungu Baba awe yote katika vyote. 29 Au
pia watafanya nini wale waliobatizwa kwa ajili ya wafu? Kama wafu hawafufuliwi
kabisa, kwa nini tena wanabatizwa kwa ajili yao? 30 Na kwa nini tuko katika hatari
kila saa? 31 Kaka na dada zangu, kupitia kujisifu kwangu katika ninyi, ambayo ninayo
katika Kristo Yesu Bwana wetu, natangaza hivi: nakufa kila siku. 32 Inanifaidia nini,
katika mtazamo wa wanadamu, kama nilipigana na wanyama wakali huko Efeso,
kama wafu hawafufuliwi? “Acha basi tule na kunywa, kwa kuwa kesho tunakufa.”
33 Msidanganywe: “Makundi mabaya huharibu tabia njema. 34 “Muwe na kiasi!
muishi katika haki! msiendelee kutenda dhambi. Kwa kuwa baadhi yenu hamna
maarifa ya Mungu. Nasema hivi kwa aibu yenu. 35 Lakini mtu mwingine atasema,
“Jinsi gani wafu wanafufuliwa? Nao watakuja na aina gani ya mwili?” 36 Wewe ni
mjinga sana! Kile ulichopanda hakiwezi kuanza kukua isipokuwa kimekufa. 37 Na
kile unachopanda sio mwili ambao utakuwa, bali ni mbegu iliyochipua. Inaweza
kuwa ngano au kitu kingine. 38 Lakini Mungu ataipa mwili kama apendavyo, na
katika kila mbengu mwili wake mwenyewe. 39 Miili yote haifanani. Isipokuwa, kuna
mwili mmoja wa wanadamu, na mwili mwingine wa wanyama, na wili mwingine
wa ndege, na mwingine kwa ajili ya samaki. 40 Pia kuna miili ya mbinguni na
miili ya duniani. Lakini utukufu wa miili ya mbinguni ni aina moja na utukufu
wa duniani ni mwingine. 41 Kuna utukufu mmoja wa jua, na utukufu mwingine
wa mwezi, na utukufu mwingine wa nyota. Kwa kuwa nyota moja inatofautiana
na nyota nyingine katika utukufu. 42 Hivyo ndivyo ulivyo pia ufufuo wa wafu.
Kinacho pandwa kinaharibika, na kinacho ota hakiharibiki. 43 Kimepandwa katika
matumizi ya kawaida, kinaoteshwa katika utukufu. Kimepandwa katika udhaifu,
kinaoteshwa katika nguvu. 44 Kimepandwa katika mwili wa asili, kinaoteshwa katika
mwili wa kiroho. Kama kuna mwili wa asili, kuna mwili wa kiroho pia. 45 Hivyo pia
imeandikwa, “Mtu wa kwanza Adamu alifanyika roho inayo ishi.” Adamu wa mwisho
alifanyika roho itoayo uhai. 46 Lakini wa kiroho hakuja kwanza bali wa asili, na kisha
wa kiroho. 47 Mtu wa kwanza ni wa dunia, alitengenezwa kwa mavumbi. Mtu wa
pili anatoka mbinguni. 48 Kama vile yule aliyetengenezwa kwa mavumbi, hivyo pia
wale waliotengenezwa kwa mavumbi. Kama vile mtu wa mbinguni alivyo, hivyo
pia wale wa mbinguni. 49 Kama ambavyo tumebeba mfano wa mtu wa mavumbi,

tutabeba pia mfano wa mtu wa mbinguni. 50 Sasa nawaambia, kaka na dada zangu,
kwamba mwili na damu haviwezi kuurithi ufalme wa Mungu. Wala wakuharibika
kurithi wakutoharibika. 51 Tazama! Nawaambia ninyi siri ya kweli: Hatutakufa
wote, bali wote tutabadilishwa. 52 Tutabadilishwa katika wakati, katika kufumba
na kufumbua kwa jicho, katika tarumbeta ya mwisho. Kwa kuwa tarumbeta italia,
na wafu watafufuliwa na hali ya kutoharibika, na tutabadilishwa. 53 Kwani huu wa
kuharibika lazima uvae wa kutoharibika, na huu wa kufa lazima uvae wa kutokufa.
54 Lakini wakati huu wa kuharibika ukivikwa wa kutokuharibika, na huu wa kufa
ukivaa wa kutokufa, ndipo utakuja msemo ambao umeandikwa, “Kifo kimemezwa
katika ushindi.” 55 “Kifo, ushindi wako uko wapi? Kifo, uko wapi uchungu wako?”
56 Uchungu wa kifo ni dhambi, na nguvu ya dhambi ni sheria. 57 Lakini shukurani
kwa Mungu, atupaye sisi ushindi kupitia Bwana wetu Yesu Kristo! 58 Kwa hiyo,
wapendwa kaka na dada zangu, iweni imara na msitikisike. Daima itendeni kazi
ya Bwana, kwa sababu mnajua kuwa kazi yenu katika Bwana siyo bure.

# 16

1 Sasa kuhusu michango kwa ajili ya waumini, kama nilivyo elekeza makanisa
ya Galatia, vivyo hivyo mwapaswa kufanya. 2 Katika siku ya kwanza ya wiki, kila
mmoja wenu aweke kitu fulani kando na kukihifadhi, kama muwezavyo. Fanyeni
hivyo ili kwamba kusiwe na michango wakati nikija. 3 Na nitakapofika, yeyote
mtakayemchagua, nitamtuma pamoja na barua kutoa sadaka yenu huko Yerusalem.
4 Na kama ni sahihi kwa mimi kwenda pia, watakwenda pamoja nami. 5 Lakini
nitakuja kwenu, wakati ninapitia Makedonia. Kwa kuwa nitapitia Makedonia.
6 Labda naweza kukaa nanyi au hata kumaliza majira ya baridi, ili kwamba muweze
kunisaidia katika safari yangu, popote niendako. 7 Kwa kuwa sitarajii kuwaona sasa
kwa muda mfupi. Kwani ninatumaini kukaa nanyi kwa muda fulani, kama Bwana
ataniruhusu. 8 Lakini nitakaa Efeso mpaka Pentekoste, 9 kwa kuwa mlango mpana
umefunguliwa kwa ajili yangu, na kuna maadui wengi wanipingao. 10 Sasa wakati
Timotheo akija, muoneni kwamba yuko na ninyi pasipo kuogopa, anafanya kazi ya
Bwana, kama ninavyofanya. 11 Mtu yeyote asimdharau. Mumsaidie katika njia yake
kwa amani, ili kwamba aweze kuja kwangu. Kwa kuwa ninamtarajia aje pamoja na
ndugu. 12 Sasa kuhusiana na ndugu yetu Apolo. Nilimtia moyo sana kuwatembelea
ninyi pamoja na ndugu. Lakini aliamua kutokuja kwa sasa. Hata hivyo, atakuja
wakati ana nafasi. 13 Muwe macho, simameni imara, mtende kama wanaume, muwe
na nguvu. 14 Basi yote myafanyayo yafanyike katika upendo. 15 Mnaijua kaya ya
Stefana. Mnajua kwamba walikuwa waamini wa kwanza huko Akaya, na kwamba
walijiweka wenyewe kwenye huduma ya waumini. Na sasa nawasihi, kaka na dada
zangu, 16 kuweni wanyenyekevu kwa watu kama hao, na kwa kila mtu anayesaidia
katika kazi na watenda kazi pamoja nasi. 17 Na ninafurahi kwa ujio wa Stefana,
Fotunato, na Akiko. Wamesimama mahali ambapo ninyi mgepaswa kuwa. 18 Kwa
kuwa wameifurahisha roho yangu na yenu. Kwa hiyo sasa, watambueni watu kama
hawa. 19 Makanisa ya Asia wametuma salamu kwenu. Akila na Priska wanawasalimu
katika Bwana, pamoja na kanisa lililoko nyumbani kwao. 20 Kaka na dada zangu wote
wanawasalimu. Salimianeni kwa busu takatifu. 21 Mimi, Paulo, naandika hivi kwa
mkono wangu. 22 Kama yeyote hampendi Bwana, basi laana iwe juu yake. Bwana
wetu, njoo! 23 Neema ya Bwana Yesu iwe nanyi. 24 Upendo wangu uwe pamoja nanyi
katika Kristo Yesu.

# 2 Wakorintho

1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu, na Timotheo ndugu yetu,
kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, na kwa waumini wote walioko katika mkoa
wote wa Akaya. 2 Neema na iwe kwenu na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu na
Bwana Yesu Kristo. 3 Na asifiwe Mungu na Baba wa Bwana Yesu Kristo. Yeye ni Baba
wa rehema na Mungu wa faraja yote. 4 Mungu hutufariji sisi katika mateso yetu yote,
ili kwamba tuweze kuwafariji wale walio katika mateso. Tunawafariji wengine kwa
faraja ileile ambayo Mungu alitumia kutufariji sisi. 5 Kwa kuwa kama vile mateso ya
Kristo huongezeka kwa ajili yetu, vile vile faraja yetu huongezeka kupitia Kristo.
6 Lakini kama tunataabishwa, ni kwa ajili ya faraja yenu na wokovu wenu. Na
kama tunafarijiwa, ni kwa ajili ya faraja yenu. Faraja yenu inafanya kazi kikamilifu
mnaposhiriki mateso kwa uvumilivu kama sisi pia tunavyoteseka. 7 Na ujasiri wetu
juu yenu ni thabiti. Tunajua kwamba kama vile ambavyo mnashiriki mateso, vile
vile mnashiriki faraja. 8 Kwa kuwa hatutaki ninyi muwe wajinga, ndugu, kuhusu
matatizo tuliyokuwa nayo huko Asia. Tulionewa zaidi ya vile tuwezavyo kubeba,
kana kwamba hatukuwa hata na tumaini la kuishi tena. 9 Kweli, tulikuwa na hukumu
ya kifo juu yetu. Lakini hiyo ilikuwa ni kutufanya sisi tusiweke tumaini juu yetu
wenyewe, badala yake tuweke tumaini katika Mungu, afufuaye wafu. 10 Alituokoa
sisi kutoka hayo maafa ya mauti, na atatuokoa tena. Tumeweka ujasiri wetu katika
yeye ya kwamba atatuokoa tena. 11 Atafanya hivi kama vile ninyi pia mtusaidiavyo
kwa maombi yenu. Hivyo wengi watatoa shukurani kwa niaba yetu kwa ajili ya
upendeleo wa neema tuliyopewa sisi kupitia maombi ya wengi. 12 Tunajivunia
hili: ushuhuda wa dhamiri yetu. Kwa kuwa ni katika nia safi na usafi wa Mungu
kwamba tulienenda wenyewe katika dunia. Tumefanya hivi hasa na ninyi, na
sio katika hekima ya ulimwengu, lakini badala yake ni katika neema ya Mungu.
13 Hatuwaandikii chochote ambacho hamwezi kukisoma au kuelewa. Ninaujasiri
14 kwamba kwa sehemu mumekwisha kutuelewa. Na ninaujasiri kwamba katika
siku ya Bwana Yesu tutakuwa sababu yenu kwa ajili ya kiburi chenu, kama vile
mtakavyokuwa kwetu. 15 Kwa sababu nilikuwa na ujasiri kuhusu hili, nilitaka kuja
kwenu kwanza, ili kwamba muweze kupokea faida ya kutembelewa mara mbili.
16 Nilikuwa napanga kuwatembelea wakati nikielekea Makedonia. Tena nilitaka
kuwatembelea tena wakati nikirudi kutoka Makedonia, na kisha ninyi kunituma
mimi wakati nikielekea Uyahudi. 17 Nilipokuwa nafikiria namna hii, je, nilikuwa
nasitasita? Je ninapanga mambo kulingana na viwango vya kibinadamu, ili kwamba
niseme “Ndiyo, ndiyo” na “Hapana, hapana” kwa wakati mmoja? 18 Lakini kama
vile Mungu alivyo mwaminifu, hatusemi vyote “Ndiyo” na “Hapana.” 19 Kwa kuwa
mwana wa Mungu, Yesu Kristo, ambaye Silvano, Timotheo na mimi tulimtangaza
miongoni mwenu, siyo “Ndiyo” na “Hapana.” Badala yake, yeye wakati wote
ni “Ndiyo.” 20 Kwa kuwa ahadi zote za Mungu ni “Ndiyo” katika yeye. Hivyo
pia kupitia yeye tunasema “Amina” kwa utukufu wa Mungu. 21 Sasa ni Mungu
ambaye hututhibitisha sisi pamoja nanyi katika Kristo, na alitutuma sisi. 22 Aliweka
muhuri juu yetu na alitupa Roho katika mioyo yetu kama dhamana ya kile ambacho
angetupatia baadaye. 23 Badala yake, namsihi Mungu kunishuhudia mimi kwamba
sababu iliyonifanya nisije Korintho ni kwamba nisiwalemee ninyi. 24 Hii sio kwa
sababu tunajaribu kudhibiti jinsi imani yenu inavyotakiwa kuwa. Badala yake,
tunafanya pamoja nanyi kwa ajili ya furaha yenu, kama mnavyosimama katika imani
yenu.

# 2

[1] Kwa hiyo niliamua kwa sehemu yangu mwenyewe kwamba nisingekuja tena
kwenu katika hali ya uchungu. [2] Kama niliwasababishia ninyi maumivu, ni nani
angenifurahisha mimi, lakini ni yule ambaye aliumizwa na mimi? [3] Niliandika
kama nilivyofanya ili kwamba wakati nikija kwenu nisiweze kuumizwa na wale
ambao wangekuwa wamenifanya nifurahi. Ninao ujasiri kuhusu ninyi nyote kwamba
furaha yangu ni furaha ile ile mliyonayo ninyi nyote. [4] Kwa kuwa niliwaandikia
ninyi kutokana na mateso makubwa, na dhiki ya moyo, na kwa machozi mengi.
Sikutaka kuwasababishia ninyi maumivu. Badala yake, nilitaka mjue upendo wa kina
nilionao kwa ajili yenu. [5] Kama kuna yeyote amesababisha maumivu, hajasababisha
tu kwangu, lakini kwa kiwango fulani - bila kuweka ukali zaidi - kwenu ninyi
nyote. [6] Hii adhabu ya mtu huyo kwa wengi inatosha. [7] Kwa hiyo sasa badala
ya adhabu, mnapaswa kumsamehe na kumfariji. Fanyeni hivi ili kwamba asiweze
kushindwa na huzuni iliyozidi. [8] Kwa hiyo ninawatia moyo kuthibitisha upendo
wenu hadharani kwa ajili yake. [9] Hii ndiyo sababu niliandika, ili kwamba niweze
kuwajaribu na kujua kuwa kama ni watii katika kila kitu. [10] Kama mkimsamehe
yeyote, na mimi pia namsamehe mtu huyo. Kile nilicho kisamehe - kama nimesamehe
chochote-kimesamehewa kwa faida yenu katika uwepo wa Kristo. [11] Hii ni kwamba
Shetani asije akatufanyia madanganyo. Kwa kuwa sisi sio wajinga kwa mipango
yake. [12] Mlango ulifunguliwa kwangu na Bwana nilipokuja kwenye mji wa Troa
kuhubiri injili ya Kristo pale. [13] Hata hivyo, sikuwa na amani ya moyo, kwa
sababu sikumkuta ndugu yangu Tito pale. Hivyo niliwaacha na nikarudi Makedonia.
[14] Lakini ashukuriwe Mungu, ambaye katika Kristo mara zote hutuongoza sisi katika
ushindi. Kupitia sisi husambaza harufu nzuri ya maarifa yake mahala pote. [15] Kwa
kuwa sisi kwa Mungu, ni harufu nzuri ya Kristo, wote kati ya wale waliookolewa na
kati ya wale wanaoangamia. [16] Kwa watu ambao wanaangamia, ni harufu kutoka
kifo hadi kifo. Kwa wale wanaookolewa, ni harufu nzuri kutoka uzima hadi uzima.
Ni nani anayestahili vitu hivi? [17] Kwa kuwa sisi sio kama watu wengi wanaouza neno
la Mungu kwa faida. Badala yake, kwa usafi wa nia, tunanena katika Kristo, kama
vile tunavyotumwa kutoka kwa Mungu, mbele ya Mungu.

# 3

[1] Je, tumeanza kujisifia wenyewe tena? Hatuhitaji barua ya mapendekezo kwenu
au kutoka kwenu, kama baadhi ya watu, je twahitaji? [2] Ninyi wenyewe ni barua yetu
ya mapendekezo, iliyoandikwa kwenye mioyo yetu, inayojulikana na kusomwa na
watu wote. [3] Na mnaonesha kwamba ninyi ni barua kutoka kwa Kristo, iliyotolewa
na sisi. Iliandikwa siyo kwa wino bali kwa Roho wa Mungu aliye hai. Haikuandikwa
juu ya vibao vya mawe, bali juu ya vibao vya mioyo ya wanadamu. [4] Na huu ndiyo
ujasiri tulio nao katika Mungu kupitia Kristo. [5] Hatujiamini wenyewe kwa kudai
chochote kama kutoka kwetu. Badala yake, kujiamini kwetu kunatoka kwa Mungu.
[6] Ni Mungu ambaye alitufanya tuweze kuwa watumishi wa agano jipya. Hili ni agano
sio la barua bali ni la Roho. Kwa kuwa barua huua, lakini roho inatoa uhai. [7] Sasa
kazi ya kifo iliyokuwa imechongwa katika herufi juu ya mawe ilikuja kwa namna
ya utukufu kwamba watu wa Israeli hawakuangalia moja kwa moja kwenye uso
wa Musa. Hii ni kwa sababu ya utukufu wa uso wake, utukufu ambao ulikuwa
unafifia. [8] Je, kazi ya Roho haitakuwa na utukufu zaidi? [9] Kwa kuwa kama huduma ya
hukumu ilikuwa na utukufu, ni mara ngapi zaidi huduma ya haki huzidi sana katika
utukufu! [10] Ni kweli kwamba, kile kilichofanywa utukufu kwanza hakina utukufu
tena katika heshima hii, kwa sababu ya utukufu unaouzidi. [11] Kwa kuwa kama kile
ambacho kilikuwa kinapita kilikuwa na utukufu, ni kwa kiasi gani zaidi kile ambacho

ni cha kudumu kitakuwa na utukufu! [12] Kwa kuwa tunajiamini hiyo, tunaujasiri sana.
[13] Hatuko kama Musa, aliyeweka utaji juu ya uso wake, ili kwamba watu wa Israel
wasiweze kuangalia moja kwa moja kwenye mwisho wa utukufu ambao ulikuwa
unatoweka. [14] Lakini fahamu zao zilikuwa zimefungwa. Hata mpaka siku hii utaji
uleule bado unabaki juu ya usomaji wa agano la kale. Haijawekwa wazi, kwa sababu
ni katika Kristo pekee inaondolewa mbali. [15] Lakini hata leo, wakati wowote Musa
asomwapo, utaji hukaa juu ya mioyo yao. [16] Lakini mtu anapogeuka kwa Bwana,
utaji unaondolewa. [17] Sasa Bwana ni Roho. Palipo na Roho wa Bwana, kuna uhuru.
[18] Sasa sisi sote, pamoja na nyuso zisizo wekewa utaji, huona utukufu wa Bwana.
Tunabadilishwa ndani ya muonekano uleule wa utukufu kutoka shahada moja ya
utukufu kwenda nyingine, kama ilivyo kutoka kwa Bwana, ambaye ni Roho.

# 4

[1] Kwa hiyo, kwa sababu tuna huduma hii, na kama ambavyo tumeipokea rehema,
hatukati tamaa. [2] Badala yake, tumekataa njia zote za aibu na zilizofichika. Hatuishi
kwa hila, na hatulitumii vibaya neno la Mungu. Kwa kuwasilisha iliyo kweli,
tunajionyesha wenyewe kwa dhamiri ya kila mtu mbele ya Mungu. [3] Lakini kama
injili yetu imefichika, imefichika kwa wale tu wanaoangamia. [4] Katika uchaguzi
wao, mungu wa ulimwengu huu amewapofusha fahamu zao zisizoamini. Matokeo
yake, hawawezi kuona nuru ya injili ya utukufu wa Kristo, ambaye ni mfano wa
Mungu. [5] Kwa kuwa hatujitangazi wenyewe, bali Kristo Yesu kama Bwana, na sisi
wenyewe kama watumishi wenu kwa ajili ya Yesu. [6] Kwa kuwa Mungu ndiye ambaye
aliyesema, “Mwanga utaangaza toka gizani.” Ameangaza katika mioyo yetu, kutoa
mwanga wa maarifa ya utukufu wa Mungu katika uwepo wa Yesu Kristo. [7] Lakini
tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili kwamba ieleweke kuwa nguvu kuu
sana ni ya Mungu na sio yetu. [8] Tunataabika katika kila hali, lakini hatusongwi.
Twaona shaka lakini hatujawi na kukata tamaa. [9] Tunateswa lakini hatujatelekezwa.
Twatupwa chini lakini hatuangamizwi. [10] Siku zote tunabeba katika mwili wetu kifo
cha Yesu, ili kwamba uzima wa Yesu uonekane pia katika miili yetu. [11] Sisi tulio
hai siku zote tumetolewa kufa kwa ajili ya Yesu, ili kwamba uhai wa Yesu uonekane
katika miili yetu ya kibinadamu. [12] Kwa sababu hii, kifo kinafanya kazi ndani yetu,
bali uzima unafanya kazi ndani yenu. [13] Lakini tuna roho ileile ya imani kulingana na
kile kilicho andikwa: “Niliamini, na hivyo nilinena.” Sisi pia tunaamini, na hivyo pia
tunanena. [14] Tunajua kuwa yule aliye mfufua Bwana Yesu pia atatufufua sisi pamoja
naye. Tunajua kuwa atatuleta sisi pamoja nanyi katika uwepo wake. [15] Kila kitu ni
kwa ajili yenu ili kwamba, kwa kadri neema inavyo enea kwa watu wengi, shukurani
zizidi kuongezeka kwa utukufu wa Mungu. [16] Hivyo hatukati tamaa. Japokuwa kwa
nje tunachakaa, kwa ndani tunafanywa upya siku hadi siku. [17] Kwa kipindi hiki
kifupi, mateso haya mepesi yanatuandaa sisi kwa ajili ya umilele mzito wa utukufu
uzidio vipimo vyote. [18] Kwa kuwa hatutazami kwa ajili ya vitu ambavyo vinaonekana,
bali kwa ajili ya vitu visivyoonekana. Vitu tunavyoweza kuviona ni vya muda tu, bali
vitu ambayo havionekani ni vya milele.

# 5

[1] Tunajua kwamba kama maskani ya ulimwenguni ambayo tunaishi humo
yanaharibiwa, tunalo jengo kutoka kwa Mungu. Ni nyumba isiyotengenezwa kwa
mikono ya wanadamu, bali ni nyumba ya milele, katika mbingu. [2] Kwa kuwa katika
hema hii tunaugua, tukitamani kuvikwa kwa maskani yetu mbinguni. [3] Tunatamani
kwa ajili ya hii kwa sababu kwa kuivaa hatutaonekana kuwa tu uchi. [4] Kwa hakika
wakati tuko ndani ya hema hii, twaugua tukilemewa. Hatutaki kuvuliwa. Badala

yake, tunataka kuvalishwa, ili kwamba kile kilicho kufa kiweze kumezwa na uzima.
5 Yule aliyetuandaa sisi kwa kitu hiki ni Mungu, ambaye alitupa sisi Roho kama ahadi
ya kile kitakacho kuja. 6 Kwa hiyo muwe na ujasiri siku zote. Muwe macho kwamba
wakati tuko nyumbani katika mwili, tuko mbali na Bwana. 7 Kwa kuwa tunatembea
kwa imani, sio kwa kuona. Kwa hiyo tunaujasiri. 8 Ni bora tuwe mbali kutoka kwenye
mwili na nyumbani pamoja na Bwana. 9 Kwa hiyo tunaifanya kuwa lengo letu, kama
tukiwa nyumbani au mbali, tumpendeze yeye. 10 Kwa kuwa lazima wote tuonekane
mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kwamba kila mmoja aweze kupokea kile
kinachostahili kwa mambo yaliyofanyika katika mwili, ikiwa ni kwa uzuri au kwa
ubaya. 11 Kwa hiyo, kwa kuijua hofu ya Bwana, tunawashawishi watu. Jinsi tulivyo,
inaonekana wazi na Mungu. Ninatumaini kuwa inaeleweka pia kwenye dhamiri
zenu. 12 Hatujaribu kuwashawishi ninyi tena kutuona sisi kama wakweli. Badala
yake, tunawapa ninyi sababu ya kujivuna kwa ajili yetu, ili kwamba muweze kuwa
na jibu kwa wale wanaojivunia kuhusu mwonekano lakini sio kile kilicho ndani ya
moyo. 13 Kwa kuwa ikiwa kama tumerukwa na akili, ni kwa ajili ya Mungu. Na
kama tuko kwenye akili zetu timamu, ni kwa ajili yenu. 14 Kwa kuwa upendo wa
Kristo watushurutisha, kwa sababu tuna uhakika na hili: kuwa mtu mmoja alikufa
kwa ajili ya wote, na kwa hiyo wote wamekufa. 15 Na Kristo alikufa kwa ajili ya
wote, ili kwamba wale wanaoishi wasiishi tena kwa ajili yao wenyewe. Badala
yake, lazima waishi kwa ajili yake yeye ambaye alikufa na alifufuliwa. 16 Kwa
sababu hii, kuanzia sasa na kuendelea hatumuhukumu mtu kulingana na viwango
vya wanadamu, ingawa hapo kwanza tulimtazama Kristo katika namna hii. Lakini
sasa hatumuhukumu yeyote kwa namna hii tena. 17 Kwa hiyo, ikiwa mtu yeyote
yuko ndani ya Kristo, yeye ni kiumbe kipya. Mambo ya kale yamepita. Tazama,
yamekuwa mapya. 18 Vitu vyote hivi vyatoka kwa Mungu. Alitupatanisha sisi kwake
mwenyewe kupitia Kristo, na ametupatia huduma ya upatanisho. 19 Hiyo ni kusema,
katika Kristo, Mungu anaupatanisha ulimwengu kwake mwenyewe, sio kuhesabu
makosa yao dhidi yao. Anawekeza kwetu ujumbe wa upatanisho. 20 Kwa hiyo
tunateuliwa kama wawakilishi wa Kristo, kana kwamba Mungu alikuwa anafanya
rufaa yake kupitia sisi. Tunawasihi ninyi kwa ajili ya Kristo: "Mpatanishwe kwa
Mungu!" 21 Alimfanya Kristo kuwa sadaka kwa ajili ya dhambi zetu. Yeye ndiye
ambaye hakutenda dhambi. Alifanya hivi ili tuweze kufanyika haki ya Mungu katika
yeye.

# 6

1 Na kwa hiyo, kufanya kazi pamoja, tunawasihi ninyi msiipokee neema ya Mungu
pasipo matokeo. 2 Kwa kuwa anasema, "Wakati uliokubalika nilikuwa makini kwenu,
na katika siku ya wokovu niliwasaidia." Tazama, sasa ni wakati uliokubalika.
Tazama, sasa ni siku ya wokovu. 3 Hatuweki jiwe la kizuizi mbele ya mtu yeyote, kwa
kuwa hatuitakii huduma yetu iletwe katika sifa mbaya. 4 Badala yake, tunajihakiki
wenyewe kwa matendo yetu yote, kwamba tu watumishi wa Mungu. Tu watumishi
wake katika wingi wa ustahimilivu, mateso, dhiki, ugumu wa maisha, 5 kupigwa,
vifungo, ghasia, katika kufanya kazi kwa bidii, katika kukosa usingizi usiku, katika
njaa, 6 katika usafi, maarifa, uvumilivu, wema, katika Roho Mtakatifu, katika upendo
halisi. 7 Tu watumishi wake katika neno la kweli, katika nguvu ya Mungu. Tuna
silaha ya haki kwa ajili ya mkono wa kuuume na wa kushoto. 8 Tunafanya kazi
katika heshima na kudharauliwa, katika kashfa na sifa. Tunatuhumiwa kuwa
wadanganyifu na wakati tu wakweli. 9 Tunafanya kazi kana kwamba hatujulikani
na bado tunajulikana vizuri. Tunafanya kazi kama wanaokufa na -Tazama! - bado
tunaishi. Tunafanya kazi kama tunaoadhibiwa kwa ajili ya matendo yetu lakini

sio kama waliohukumiwa hata kufa. 10 Tunafanya kazi kama wenye masikitiko,
lakini siku zote tuna furaha. Tunafanya kazi kama maskini, lakini tunatajirisha
wengi. Tunafanya kazi kana kwamba hatupati kitu bali kama tunaomiliki kila kitu.
11 Tumezungumza ukweli wote kwenu, Wakorintho, na mioyo yetu imefunguka kwa
upana. 12 mioyo yenu haizuiliwi na sisi, bali mnazuiliwa na hisia zenu wenyewe.
13 Sasa katika kubadilishana kwa haki - ninaongea kama kwa watoto - fungueni mioyo
yenu kwa upana. 14 Msifungamanishwe pamoja na wasioamini. Kwa kuwa kuna
uhusiano gani kati ya haki na uasi? Na kuna ushirika gani kati ya nuru na giza?
15 Ni makubaliano gani Kristo anaweza kuwa nayo na Beliari? Au yeye aaminiye
ana sehemu gani pamoja na asiyeamini? 16 Na kuna makubaliano gani yapo kati ya
hekalu la Mungu na sanamu? Kwa kuwa sisi ni hekalu la Mungu aliye hai, kama
ambavyo Mungu alisema: “Nitakaa kati yao na kutembea kati yao. Nitakuwa Mungu
wao, nao watakuwa watu wangu.” 17 Kwa hiyo, “Tokeni kati yao, na mkatengwe nao,”
asema Bwana. “Msiguse kitu kichafu, na nitawakaribisha ninyi. 18 Nitakuwa Baba
kwenu, nanyi mtakuwa wanangu wa kiume na wa kike,” asema Bwana Mwenyezi.

# 7

1 Wapendwa wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizi, na tujitakase wenyewe kwa
kila jambo ambalo linatufanya kuwa wachafu katika miili yetu na katika roho.
Na tuutafute utakatifu katika hofu ya Mungu. 2 Fanyeni nafasi kwa ajili yetu!
Hatujamkosea mtu yeyote. Hatukumdhuru mtu yeyote. Hatujajinufaisha kwa faida
ya mtu yeyote. 3 Nasema hili siyo kwa kuwalaumu. Kwa kuwa nimeshasema kwamba
mmo mioyoni mwetu, kwetu sisi kufa pamoja na kuishi pamoja. 4 Nina ujasiri mwingi
ndani yenu, na ninajivuna kwa ajili yenu. Nimejawa na faraja. Ninajawa na furaha
hata katikati ya mateso yetu yote. 5 Tulikuja Makedonia, miili yetu haikuwa na
pumziko. Badala yake, tulipata taabu kwa namna zote kwa kupigwa vita upande wa
nje na hofu upande wa ndani. 6 Lakini Mungu, anayefariji waliokata tamaa, alitufariji
kwa ujio wa Tito. 7 Haikuwa kwa ujio wake tu kwamba Mungu alitufariji. ilikuwa
pia faraja zile Tito alizopokea kutoka kwenu. Yeye alituambia upendo mkuu mlionao,
huzuni yenu, na mlivyokuwa na wasiwasi kwa ajili yangu. Hivyo nimezidi kuwa
na furaha zaidi. 8 Hata ingawa waraka wangu uliwafanya kusikitika, mimi siujutii.
lakini ninaujutia wakati nilipoona waraka huo uliwafanya ninyi kuwa na huzuni.
lakini mlikuwa na huzuni kwa muda mfupi. 9 Sasa nina furaha, si kwa sababu
mlikuwa na shida, lakini kwa sababu huzuni zenu iliwaleta kwenye toba. Mlipatwa
na huzuni ya kiungu, hivyo mliteswa si kwa hasara kwa sababu yetu. 10 Kwa kuwa
huzuni ya kiungu huleta toba ambayo hukamilisha wokovu bila ya kuwa na majuto.
Huzuni ya kidunia, hata hivyo, huleta mauti. 11 Angalieni huzuni hii ya kiungu
ilizalisha azma gani kubwa ndani yenu. Jinsi gani azma ilikuwa kubwa ndani yenu
kuthibitisha kuwa hamkuwa na hatia. Kwa jinsi gani uchungu wenu ulivyokuwa
mkubwa, hofu yenu, matamanio yenu, bidii yenu, na shauku yenu kuona kwamba
haki inapaswa kutendeka! Katika kila jambo mmethibitisha wenyewe kutokuwa na
hatia. 12 Ingawa niliwaandikia ninyi, sikuandika kwa ajili ya mkosaji, wala si kwa mtu
aliyeteswa na maovu. Nimeandika ili kwamba udhati wa mioyo yenu kwa ajili yetu
ifanywe kujulikana kwenu mbele ya macho ya Mungu. 13 Ni kwa ajili ya hii kwamba
tunafarijika. Katika nyongeza ya faraja yetu wenyewe, tunafurahi pia, hata zaidi kwa
sababu ya furaha ya Tito, kwa kuwa roho yake iliburudishwa na ninyi nyote. 14 Kwa
kuwa kama nilijivuna kwake kuhusiana na ninyi, sikuwa na aibu. Kinyume chake,
kama tu kila neno tulilolisema kwenu lilikuwa kweli, Majivuno yetu kuhusu ninyi
kwa Tito yalithibitisha kuwa kweli. 15 Upendo wake kwa ajili yenu hata ni mkubwa

zaidi, kama akumbukapo utii wenu nyote, jinsi mlivyomkaribisha yeye kwa hofu na
kutetemeka. 16 Ninafurahi kwa sababu nina ujasiri kamili ndani yenu.

# 8

1 Tunawataka ninyi mjue, kaka na dada, kuhusu neema ya Mungu ambayo
imetolewa kwa makanisa ya Makedonia. 2 Wakati wa jaribu kubwa la mateso, wingi
wa furaha yao na ongezeko la umaskini wao umezaa utjiri mkubwa wa ukarimu.
3 Kwa maana nashuhudia kwamba walitoa kwa kadiri ya walivyoweza, na hata zaidi
ya walivyoweza. 4 Na kwa hiari yao wenyewe kwa kutusihi kwingi, walituomba
kwa ajili ya kushiriki katika huduma hii kwa waumini. 5 Hii haikutokea kama
tulivyokuwa tunatarajia. Badala yake, kwanza walijitoa wao wenyewe kwa Bwana.
Kisha wakajitoa wao wenyewe kwetu kwa mapenzi ya Mungu. 6 Hivyo tulimsihi
Tito, aliyekuwa tayari ameanzisha kazi hii, kuleta katika utimilifu tendo hili la
ukarimu juu yenu. 7 Lakini ninyi mna wingi katika kila kitu- katika imani, katika
usemi, katika maarifa, katika bidii, na katika upendo wenu kwa ajili yetu. Hivyo
hakikisheni kwamba ninyi mnakuwa na wingi pia katika tendo hili la ukarimu.
8 Nasema hili si kama amri. Badala yake, nasema hili ili kupima uhalisi wa upendo
wenu kwa kuulinganisha na shauku ya watu wengine. 9 Kwa maana mnajua neema
ya Bwana wetu Yesu Kristo. Hata kama alikuwa tajiri, kwa ajili yenu alikuwa
maskini. Ili kwamba kupitia umaskini wake mweze kuwa tajiri. 10 Katika jambo
hili nitawapa ushauri ambao utawasaidia. Mwaka mmoja uliopita, hamkuanza
tuu kufanya jambo. Lakini mlitamani kulifanya. 11 Sasa likamilisheni. Kama tu
kulivyokuwa na shauku na nia ya kulifanya, kisha, je, mngeweza pia kulileta katika
ukamilifu, kwa kadri ya mnavyoweza. 12 Kwa kuwa mnashauku ya kufanya tendo
hili, ni jambo zuri na linakubalika. Lazima lisimame juu ya kile alichonacho mtu,
siyo juu ya asichokuwa nacho mtu. 13 Kwa kuwa kazi hii siyo kwa ajili kwamba
wengine waweze kupata nafuu na ninyi mweze kulemewa. Badala yake, kuwe
na usawa. 14 Wingi wenu wa wakati wa sasa utasaidia kwa kile wanachohitaji.
Hii ni hivyo pia ili kwamba wingi wao uweze kusaidia mahitaji yenu, na kwamba
kuwe na usawa. 15 Hii ni kama ilivyoandikwa; “Yeye aliye na vingi hakuwa na
kitu chochote kilichobaki na yeye aliyekuwa na kidogo hakuwa na uhitaji wowote.”
16 Lakini ashukuriwe Mungu, aliyeweka ndani ya moyo wa Tito moyo uleule wa bidii
ya kujali ambyo ninayo kwa ajili yenu. 17 Kwa kuwa si tu alipokea maombi yetu,
bali pia alikuwa na bidii kuhusiana na maombi hayo. Alikuja kwenu kwa hiari
yake mwenyewe. 18 Tumemtuma pamoja naye ndugu ambaye anasifiwa miongoni
mwa makanisa kwa ajili ya kazi yake katika kutangaza injili. 19 Si hivi tu, lakini
pia alichaguliwa na makanisa kusafiri nasisi katika kulibeba sehemu mbalimbali
tendo hili la ukarimu. Hii ni kwa utukufu wa Bwana mwenyewe na kwa shauku
yetu ya kusaidia. 20 Tunaepuka uwezekano kwamba yeyote napaswa kulalamika
kuhusiana na sisi kuhusiana na ukarimu huu ambao tunaubeba. 21 Tunachukua
uangalifu kufanya kilicho cha heshima, sio tu mbele za Bwana, lakini pia mbele za
watu. 22 Pia tunamtuma ndugu mwingine pamoja nao. Tumempima mara nyingi,
na tumemwona ni mwenye shauku for ajili ya kazi nyingi. Hata sasa ana bidii
zaidi kwa sababu ya ujasiri mkubwa alionao ndani yenu. 23 Kwa habari ya Tito,
yeye ni mshirika mwenza wangu na mtendakazi mwenzangu kwa ajili yenu. Kama
kwa ndugu zetu, wanatumwa na makanisa. Ni waheshima kwa Kristo. 24 Hivyo,
waonesheni upendo wenu, na muoneshe kwa makanisa sababu ya majivuno yetu
kwa ajili yenu.

# 9

1 Kuhusiana na huduma kwa ajili ya waumini, ni bora zaidi kwangu kuwaandikia.
2 Ninajua kuhusu shauku yenu, ambayo nilijivunia kwa watu wa Makedonia.
Niliwaambia kwamba Akaya imekuwa tayari tangu mwaka uliopita. Hamu yenu
imewatia moyo wengi wao kutenda. 3 Sasa, nimewatuma ndugu ili kwamba
majivuno yetu kuhusu ninyi yasiwe ya bure, na ili kwamba mngekuwa tayari,
kama nilivyosema mngekuwa. 4 Vinginevyo, kama mtu yeyote wa Makedonia akija
pamoja nami na kuwakuta hamjawa tayari, tungeona haya — sisemi chochote kuhusu
ninyi—kwa kuwa jasiri sana katika ninyi. 5 Hivyo niliona ilikuwa muhimu kuwasihi
ndugu kuja kwenu na kufanya mipango mapema kwa ajili ya zawadi mlizoahidi.
Hii ni hivyo ili kwamba ziwe tayari kama baraka, na si kama kitu kilichoamriwa.
6 Wazo ni hili: mtu apandaye haba pia atavuna haba, na yeyote apandaye kwa
lengo la baraka pia atavuna baraka. 7 Basi na kila mmoja atoe kama alivyopanga
moyoni mwake. Basi naye asitoe kwa huzuni au kwa kulazimishwa. Kwa kuwa
Mungu humpenda yule atoaye kwa furaha. 8 Na Mungu anaweza kuizidishia kila
baraka kwa ajili yenu, ili kwamba, kila wakati, katika mambo yote, muweze kupata
yote mnayohitaji. Hii itakuwa ili kwamba mueze kuzidisha kila tendo jema. 9 Ni
kama ilivyoandikwa: "Ametapanya utajiri wake na kuutoa kwa maskini. Haki yake
yadumu milele." 10 Naye atoaye mbegu kwa mpanzi na mkate kwa ajili ya chakula,
pia atatoa na kuzidisha mbegu yenu kwa ajili ya kupanda. Yeye ataongeza mavuno
ya haki yenu. 11 Mtatajirishwa kwa kila namna ili kwamba muweze kuwa wakarimu.
Hii italeta shukrani kwa Mungu kupitia sisi. 12 Kwa kufanya huduma hii sio tu
inagusa mahitaji ya waumini. Pia huzidisha katika matendo mengi ya shukrani kwa
Mungu. 13 Kwa sababu ya kupimwa kwenu na kuthibitishwa kwa huduma hii, pia
mtamtukuza Mungu kwa utii kwa ukiri wenu wa injili ya Kristo. Pia mtamtukuza
Mungu kwa ukarimu wa karama yenu kwao na kwa kila mmoja. 14 Wanawatamani,
na wanaomba kwa ajili yenu. Wanafanya hivi kwa sababu ya neema kubwa ya
Mungu iliyo juu yenu. 15 Shukrani ziwe kwa Mungu kwa karama yake isiyoelezeka!

# 10

1 Mimi Paulo, mwenyewe nawasihi kwa unyenyekevu na upole wa Kristo. Mimi
ni mpole wakati nikiwa mbele yenu, Lakini ninaujasiri kwenu wakati nikiwa mbali
nanyi. 2 Nawaomba ninyi kwamba, wakati nikiwepo pamoja nanyi, sitahitaji kuwa
jasiri na kujiamini kwangu mwenyewe. Lakini nafikiri nitahitaji kuwa jasiri wakati
nikiwapinga wale wanaodhani kwamba tunaishi kwa jinsi ya mwili. 3 Kwa kuwa
hata kama tunatembea katika mwili, hatupigani vita kwa jinsi ya mwili. 4 Kwa kuwa
silaha tunazotumia kupigana si za kimwili. Badala yake, zina nguvu ya kiungu ya
kuharibu ngome. Zinaondosha kabisa mijadara inayopotosha. 5 Pia, tunaharibu
kila chenye mamlaka kijiinuacho dhidi ya maarifa ya Mungu. Tunalifanya mateka
kila wazo katika utii kwa Kristo. 6 Na tunapata utayari wa kuadhibu kila matendo
lisilo na utii, mara tu utii wenu unapokuwa kamili. 7 Tazama kile kilichowazi
mbele yenu. Kama yeyote anashawishika kwamba yeye ni wa Kristo, na hebu
ajikumbushe yeye mwenyewe kwamba kama tu alivyo ni wa Kristo, hivyo ndiyo
na sisi pia tuko hivyo. 8 Kwa kuwa hata nikijivuna kidogo zaidi kuhusu mamlaka
yetu, ambayo Bwana aliyatoa kwa ajili yetu kuwajenga ninyi na siyo kuwaharibu,
sitaona haya. 9 Sihitaji hili lionekane kwamba nawatisha ninyi kwa nyaraka zangu.
10 Kwa vile baadhi ya watu husema, " Nyaraka zake ni kali na zina nguvu, lakini
kimwili yeye ni dhaifu. Maneno yake hayastahili kusikilizwa." 11 Hebu watu wa
jinsi hiyo waelewe kwamba kile tusemacho kwa waraka wakati tukiwa mbali, ni
sawasawa na vile tutakavyotenda wakati tukiwa pale. 12 Hatuendi mbali mno

kama kujikusanya wenyewe au kujilinganisha wenyewe na wale ambao hujisifia
wenyewe. Lakini wanapojipima wenyewe na kila mmoja wao, hawana akili. [13] Sisi,
hata hivyo, hatutajivuna kupita mipaka. Badala yake, tutafanya hivyo tu ndani ya
mipaka ambayo Mungu ametupimia sisi, mipaka inayofika umbali kama wenu ulivyo.
[14] Kwa kuwa hatukujizidishia wenyewe tulipowafikia ninyi. Tulikuwa wa kwanza
kufika kwa umbali kama wenu kwa injili ya Kristo. [15] Hatujajivuna kupita mipaka
kuhusu kazi za wengine. Badala yake, tunatumaini kama imani yenu ikuwavyo
kwamba eneo letu la kazi litapanuliwa sana, na bado ni ndani ya mipaka sahihi.
[16] Tunatumaini kwa hili, ili kwamba tuweze kuhubiri injili hata kwenye mikoa zaidi
yenu. Hatutajivuna kuhusu kazi inayofanywa katika maeneo mengine. [17] “Lakini
yeyote ajivunaye, ajivune katika Bwana.” [18] Kwa maana siyo yule ajithibitishaye
mwenyewe anathibitishwa. Isipokuwa, ni yule ambaye Bwana humthibitisha.

## 11

[1] Nahisi kwamba mngevumiliana na mimi katika baadhi ya upumbavu. Lakini
kwa kweli mnavumiliana na mimi. [2] Kwa kuwa ni mwenye wivu kuhusu ninyi.
Nina wivu wa Mungu kwa ajili yenu, tangu nilipowaahidi ninyi kwenye ndoa ya
mume mmoja. Niliahidi kuwaleta ninyi kwa Kristo kama bikra safi. [3] Lakini
ninaogopa kwamba kwa namna fulani, kama nyoka alivyomdanganya Eva kwa hila
yake, mawazo yenu yanaweza kupotoshwa mbali kutoka kwenye ibada halisi na
safi kwa Kristo. [4] Kwa kuwa kwa mfano kwamba mtu fulani akaja na kutangaza
Yesu mwingine tofauti na yule tuliyewahubiri. Au kwa mfano kwamba mkapokea
roho mwingine tofauti na yule mliyempokea. Au kwa mfano kwamba mkapokea
injili nyingine tofauti na ile mliyoipokea. Mkavumilia mambo haya vema inatosha!
[5] Kwa kuwa nadhani kwamba mimi si miongoni mwa walio duni kwa hao wanaoitwa
mitume-bora. [6] Lakini hata kama mimi sijafundishwa katika kutoa hotuba, siko
hivyo katika maarifa. Kwa kila namna na katika mambo yote tumelifanya hili
kujulikana kwenu. [7] Je, nilifanya dhambi kwa kujinyenyekeza mwenyewe ili ninyi
muweze kuinuliwa? Kwa kuwa nilihubiri kwa uhuru injili ya Mungu kwenu.
[8] Nilinyang'anya makanisa mengine kwa kupokea msaada kutoka kwao ili kwamba
ningeweza kuwahudumia ninyi. [9] Wakati nilipokuwa nanyi na nilikuwa katika
uhitaji, sikumlemea yeyote. Kwa kuwa mahitaji yangu yalitoshelezwa na ndugu
waliokuja kutoka Makedonia. Katika kila kitu nimejizuia mwenyewe kutokuwa
mzigo kwenu, na nitaendelea kufanya hivyo. [10] Kama kweli ya Kristo ilivyo
ndani yangu, huku kujisifu kwangu, hakutanyamazishwa katika sehemu za Akaya.
[11] Kwa nini? Kwa sababu siwapendi? Mungu anajua nawapenda. [12] Lakini kile
ninachokifanya, nitakifanya pia. Nitakifanya ili kwamba niweze kuzuia nafasi ya
wale wanaotamani nafasi ya kuwa kama tulivyo katika kile kile wanachojivunia.
[13] Kwa kuwa watu wale ni mitume wa uongo na watendakazi wadanganyifu.
Wanajigeuza wenyewe kama mitume wa Kristo. [14] Na hii haishangazi, kwa kuwa
hata Shetani hujigeuza mwenyewe kama malaika wa nuru. [15] Hii haina mshangao
mkubwa kama watumishi wake pia kujigeuza wenyewe kama watumishi wa haki.
Hatma yao itakuwa kama matendo yao yastahilivyo. [16] Nasema tena: Basi na asiwepo
mtu yeyote anayefikiri mimi ni mpumbavu. Lakini kama mkifanya, nipokeeni
mimi kama mpumbavu ili niweze kujisifu kidogo. [17] Kile ninachosema kuhusu
huku kujiamini kwa kujivuna hakuhukumiwi na Bwana, lakini nazungumza kama
mpumbavu. [18] Kwa vile watu wengi hujivuna kwa jinsi ya mwili, nitajivuna pia.
[19] Kwa kuwa mlichukuliana kwa furaha na wapumbavu, ninyi wenyewe mna busara!
[20] Kwa kuwa mnachukuliana na mtu kama akikutia utumwani, kama husababisha
mgawanyiko kati yenu, kama akiwatumia ninyi kwa faida yake, kama akijiweka juu

hewani, au kama akiwapiga usoni. 21 Nitasema kwa aibu yetu kwamba sisi tukuwa
dhaifu sana kufanya hivyo. Na bado kama yeyote akijivuna— nazungumza kama
mpumbavu— mimi pia nitajivuna. 22 Je, wao ni Wayahudi? Na mimi ni hivyo. Je, wao
ni Waisraeli? Na mimi ni hivyo. Je, wao ni uzao wa Abrahamu? Na mimi ni hivyo.
23 Je, wao ni watumishi wa Kristo? {Nanena kama nilirukwa na akili zangu. } Mimi ni
zaidi. Nimekuwa hata katika kazi ngumu zaidi, mbali zaidi ya kuwa vifungoni, katika
kupigwa kupita vipimo, katika kukabili hatari nyingi za kifo. 24 Kutoka kwa Wayahudi
nimepokea mara tano "mapigo arobaini kutoa moja." 25 Mara tatu nilipigwa kwa
fimbo. Mara moja nilipigwa mawe. Mara tatu nilinusurika melini. Nimetumia
usiku na mchana katika bahari wazi. 26 Nimekuwa katika safari za mara kwa mara,
katika hatari za mito, katika hatari za majambazi, katika hatari kutoka kwa watu
wangu mwenyewe, katika hatari kutoka kwa watu wa mataifa, katika hatari ya mji,
katika hatari ya jangwa, katika hatari ya bahari, katika hatari kutoka kwa ndugu
waongo. 27 Nimekuwa katika kazi ngumu na katika maisha magumu, katika usiku
mwingi wa kutolala, katika njaa na kiu, mara nyingi katika kufunga, katika baridi
na uchi. 28 Mbali na kila kitu kingine, kuna msukumo wa kila siku juu yangu wa
wasiwasi wangu kwa ajili ya makanisa. 29 Nani ni dhaifu, na mimi siyo dhaifu? Nani
amesababisha mwingine kuanguka dhambini, na mimi siungui ndani? 30 Kama ni
lazima nijivune, nitajivunia kuhusu kile kinachoonyesha udhaifu wangu. 31 Mungu
na Baba wa Bwana Yesu, yeye ambaye anatukuzwa milele, anajua kwamba mimi
sidanganyi. 32 Kule Dameski, mkuu wa mkoa chini ya mfalme Areta alikuwa akiulinda
mji wa Dameski ili kunikamata. 33 Lakini niliwekwa kikapuni, kupitia dirishani
katika ukuta, na nikanusurika kutoka mikononi mwake.

# 12

1 Ni lazima nijivune, lakini hakuna kinachoongezwa na hilo. Bali nitaendelea
kwenye maono na mafunuo kutoka kwa Bwana. 2 Namjua mtu mmoja katika Kristo
ambaye miaka kumi na minne iliyopita ambaye—ikiwa katika mwili, au nje ya
mwili, mimi sijui, Mungu anajua—alinyakuliwa juu katika mbingu ya tatu. 3 Na
ninajua kwamba mtu huyu—ikiwa katika mwili, au nje ya mwili, mimi sijui, Mungu
anajua— 4 alichukuliwa juu hadi paradiso na kusikia mambo matakatifu sana kwa
mtu yeyote kuyasema. 5 Kwa niaba ya mtu kama huyo nitajivuna. lakini kwa niaba
yangu mwenyewe sitajivuna. Isipokuwa kuhusu udhaifu wangu. 6 Kama nikitaka
kujivuna, nisingekuwa mpumbavu, kwa kuwa ningekuwa ninazungumza ukweli.
Lakini nitaacha kujivuna, ili kwamba asiwepo yeyote atakayenifikiria zaidi ya hayo
kuliko kinachoonekana ndani yangu au kusikika kutoka kwangu. 7 Sitajivuna pia
kwa sababu ya hayo mafunuo ya aina ya ajabu. Kwa hiyo, hivyo sitajawa na kiburi,
mwiba uliwekwa ndani ya mwili wangu, mjumbe wa shetani kunishambulia mimi, ili
nisigeuke kuwa mwenye majivuno. 8 Mara tatu nilimsihi Bwana kuhusu hili, ili yeye
kuundoa kutoka kwangu. 9 Naye akaniambia, "Neema yangu inatosha kwa ajili yako,
kwa kuwa nguvu hufanywa kamili katika udhaifu. Hivyo, ningetamani zaidi kujivuna
zaidi kuhusu udhaifu wangu, ili kwamba uwezo wa Kristo uweze kukaa juu yangu.
10 Kwa hiyo ninatosheka kwa ajili ya Kristo, katika udhaifu, katika matukano, katika
shida, katika mateso, katika hali ya masikitiko. Kwa kuwa wakati nikiwa dhaifu, kisha
nina nguvu. 11 Mimi nimekuwa mpumbavu! ninyi mlinilazimisha kwa hili, kwa kuwa
ningekuwa nimesifiwa na ninyi. Kwa kuwa sikuwa duni kabisa kwa hao waitwao
mitume—bora, hata kama mimi si kitu. 12 Ishara za kweli za mtume zilifanyika
katikati yenu kwa uvumilivu, ishara na maajabu na matendo makuu. 13 Kwa namna
gani mlikuwa wa muhimu wa chini kuliko makanisa yaliyobaki, isipokuwa kwamba
sikuwa mzigo kwenu? Mnisamehe kwa kosa hili! 14 Tazama! mimi niko tayari kuja

kwenu kwa mara ya tatu. Sitakuwa mzigo kwenu, kwa kuwa sitaki kitu kilicho chenu.
Nawataka ninyi. Kwa kuwa watoto hawapaswi kuweka akiba kwa ajili ya wazazi.
Badala yake, wazazi wanapaswa kuweka akiba kwa ajili ya watoto. 15 Nitafurahi zaidi
kutumia na kutumiwa kwa ajili ya nafsi zenu. Kama ninawapenda zaidi, natakiwa
kupendwa kidogo? 16 Lakini kama ilivyo, sikuwalemea mzigo ninyi. Lakini kwa kuwa
mimi ni mwerevu sana, mimi ni yule aliyewashika ninyi kwa nimekuwa ambaye
aliyewapata kwa udanganyifu. 17 Je, nilichukua kwa kujifanyia faida kwa yeyote
niliyemtuma kwenu? 18 Nilimsihi Tito kuja kwenu, na nilituma ndugu mwingine
pamoja naye. Je, Tito aliwafanyia faida ninyi? Je, hatukutembea katika njia ile
ile? Je, hatukutembea katika nyayo zile zile? 19 Mnadhani kwa muda huu wote
tumekuwa tukijitetea sisi wenyewe kwenu? Mbele za Mungu, na katika Kristo,
tumekuwa tukisema kila kitu kwa ajili ya kuwaimarisha ninyi. 20 Kwa kuwa nina
hofu kwamba nitakapokuja naweza nisiwapate ninyi kama ninavyotamani. Nina
hofu kwamba mnaweza msinipate mimi kama mnavyotamani. Nahofia kwamba
kunaweza kuwa na majadiliano, wivu, milipuko ya hasira, tamaa ya ubinafsi,
umbeya, kiburi, na ugomvi. 21 Nina hofu kwamba nitakaporudi tena, Mungu wangu
anaweza kuninyenyekeza mbele yenu. Nina hofu kwamba ninaweza kuhuzunishwa
na wengi ambao wamefanya dhambi kabla ya sasa, na ambao hawakutubu uchafu,
na uasherati na mambo ya tamaa wanayoyatenda.

# 13

1 Hii ni mara ya tatu kwamba nakuja kwenu. "Kila shitaka lazima lijengwe
na uthibitisho wa mashahidi wawili au watatu." 2 Nimekwishashasema kwa hao
waliotenda dhambi kabla na kwa wengine wote wakati nilipokuwa huko mara ya pili,
na ninasema tena: Nitakapokuja tena, sitawavumilia. 3 Nawaambia ninyi hili kwa
sababu mnatafuta ushahidi kwamba Kristo ananena kupitia mimi. Yeye sio dhaifu
kwenu, badala yake, yeye ni mwenye nguvu ndani yenu. 4 Kwa kuwa alisulibiwa
katika udhaifu, lakini yu hai kwa nguvu za Mungu. Kwa kuwa sisi pia tu dhaifu ndani
yake, lakini tutaishi naye kwa nguvu za Mungu miongoni mwenu. 5 Jichunguzeni
wenyewe muone kama mko katika imani. Jipimeni wenyewe. Hamgundui kwamba
Yesu Kristo yu ndani yenu? Yeye yumo, vinginevyo kama hamjathibitishwa. 6 Na
nina ujasiri kwamba ninyi mtagundua kwamba sisi hatukukataliwa. 7 Sasa tunaomba
kwa Mungu kwamba msiweze kufanya chochote kibaya. Siombi kwamba sisi tuweze
kuonekana tumepita jaribu, badala yake ninaomba kwamba muweze kufanya kilicho
sahihi, Ingawa tunaweza kuonekana tumeshindwa jaribu. 8 Kwa kuwa sisi hatuwezi
kufanya lolote kinyume na kweli, lakini ni kwa ajili ya kweli tu. 9 Kwa kuwa
tunafurahi wakati tunapokuwa dhaifu nanyi mkiwa na nguvu. Tunaomba pia
kwamba muweze kufanywa wakamilifu. 10 Nayaandika mambo haya wakati nikiwa
mbali nanyi, ili kwamba wakati nikiwa pamoja nanyi sihitaji kuwaonesha ukali ninyi.
Sihitaji kutumia mamlaka Bwana aliyonipaa mimi niwajenge na siyo kuwaharibu
chini. 11 Hatimaye, ndugu wa kiume na wa kike, furahini! fanyeni kazi kwa ajili ya
urejesho, mtiwe moyo, kubalianeni ninyi kwa ninyi, muishi katika amani. Na Mungu
wa upendo na amani atakuwa pamoja nanyi. 12 Salimianeni kila mmoja kwa busu
takatifu. 13 Waumini wote wanawasalimu. 14 Neema ya Bwana Yesu Kristo, upendo
wa Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu uwe pamoja nanyi nyote.

# Wagalatia

1 Mimi ni Paulo mtume. Mimi sio mtume kutoka kwa wanadamu wala kupitia kwa
mwanadamu, lakini kupitia kwa Yesu Kristo na Mungu Baba aliyemfufua kutoka
kwa wafu. 2 Pamoja na ndugu wote na mimi, ninayaandikia makanisa ya Galatia.
3 Neema iwe kwenu na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo,
4 aliyejitoa mwenyewe kwa ajili ya dhambi zetu ili kwamba atukomboe na nyakati
hizi za uovu, kutokana na mapenzi ya Mungu wetu na Baba. 5 Kwake uwe utukufu
milele na milele. 6 Ninashangaa kwamba mnageukia haraka kwenye injili nyingine.
Ninashangaa kwamba mnageukia mbali kutoka kwake yeye aliyewaita kwa neema ya
Kristo. 7 Hakuna injili nyingine, lakini kuna baadhi ya watu wanao wasababishieni
nyinyi matatizo na kutaka kubadilisha injili ya Kristo. 8 Lakini hata kama ni sisi
au malaika kutoka mbinguni atatangaza kwenu injili tofauti na ile tuliyoitangaza
kwenu, na alaaniwe. 9 Kama tulivyo sema mwanzoni, na sasa nasema tena, “Kama
kuna mtu atawatangazia kwenu injili tofauti na mliyoipokea, na alaaniwe.” 10 Kwani
sasa hivi ninatafuta uthibitisho wa watu au Mungu? Ninatafuta kuwafurahisha
wanadamu? Kama ninaendelea kujaribu kuwafurahisha wanadamu, mimi sio
mtumishi wa Kristo. 11 Ndugu, ninataka ninyi mjue kwamba injili niliyoitangaza
haitokani na wanadamu. 12 Sikuipokea kutoka kwa mtu, wala sikufundishwa. Badala
yake, ilikuwa ni kwa ufunuo wa Yesu Kristo kwangu. 13 Mmekwisha sikia juu ya
maisha yangu ya nyuma katika dini ya Kiyahudi, jinsi nilivyokuwa nikilitesa kwa
ukali kanisa la Mungu zaidi ya kipimo na kuliteketeza. 14 Nilikuwa nimeendelea
katika Dini ya Kiyahudi zaidi ya ndugu zangu wengi Wayahudi. Nilikuwa na bidii
sana katika tamaduni za baba zangu. 15 Lakini Mungu alipendezwa kunichagua mimi
kutoka tumboni mwa mama. Aliniita mimi kupitia neema yake 16 kumdhihirisha
Mwanawe ndani yangu, ili kwamba nimtangaze yeye miongoni mwa watu wa
mataifa. Wala sikutafuta ushauri wa mwili na damu 17 na sikupanda kwenda
Yerusalem kwa wale waliokuwa mitume kabla yangu. Badala yake nilienda Uarabuni
na baadae kurudi Damesiki. 18 Kisha baada ya miaka mitatu nilipanda kwenda
Yerusalemu kumtembelea Kefa, nikakaa naye kwa siku kumi na tano. 19 Lakini
sikuona mitume wengine isipokuwa Yakobo, ndungu yake na Bwana. 20 Tazama,
mbele za Mungu, sidanganyi kwa kile niandikacho kwenu. 21 Kisha nilikwenda mikoa
ya Shamu na Kilikia. 22 Sikuwa najulikana kwa macho kwa makanisa ya Uyahudi yale
yaliyokuwa katika Kristo, 23 lakini walikuwa wakisikia tu, “Yeye aliyekuwa akitutesa
sasa anatangaza imani aliyokuwa akiiharibu.” 24 Walikuwa wakimtukuza Mungu
kwa ajili yangu.

## 2

1 Baada ya miaka kumi na nne niliendа tena Yerusalemu pamoja na Barnaba. Pia
nilimchukua Tito pamoja nami. 2 Nilienda kwa sababu Mungu alijidhihirisha kwangu
kwamba nilipaswa kwenda. Niliweka mbele yao Injili ambayo niliitangaza kwa watu
wa mataifa. (Lakini niliongea kwa siri kwa waliosemekana kuwa viongozi muhimu).
Nilifanya hivi ili kuhakikisha kwamba nilikuwa sikimbii, au nilikimbia bure. 3 Lakini
hata Tito, aliyekuwa pamoja nami, aliyekuwa Myunani, alilazimishwa kutahiriwa.
4 Jambo hili lilitokea kwa sababu ya ndugu wa uongo waliokuja kwa siri kupeleleza
uhuru tuliokuwa nao katika Kristo Yesu. Walitamani kutufanya sisi kuwa watumwa
wa sheria. 5 Hatukujitoa kuwatii hata kwa saa moja, ili kwamba injili ya kweli
ibaki bila kubadilika kwenu. 6 Lakini wale waliosemwa kuwa walikuwa viongozi

hawakuchangia chochote kwangu. Chochote walichokuwa wakikifanya hakikuwa
na maana kwangu. Mungu hakubali upendeleo wa wanadamu. 7 Badala yake,
waliniona kwamba nimeaminiwa kuitangaza injili kwa wale ambao hawakutahiriwa.
Ilikuwa kama Petro atangaze injili kwa waliotahiriwa. 8 Kwa maana Mungu,
aliyefanya kazi ndani ya Petro kwa ajili ya utume kwa wale waliotahiriwa, pia
alifanya kazi ndani yangu kwa watu wa mataifa. 9 Wakati Yakobo, Kefa, na Yohana,
waliotambulika kuwa waliojenga Kanisa, walifahamu neema niliyopewa mimi,
walitupokea katika ushirika mimi na Barnaba. Walifanya hivi ili kwamba twende
kwa watu wa mataifa, na ili kwamba waweze kwenda kwa wale waliotahiriwa. 10 Pia
walitutaka sisi kuwakumbuka masikini. Mimi pia nilikuwa natamani kufanya jambo
hili. 11 Wakati Kefa alipokuja Antiokia, nilimpinga waziwazi kwa sababu alikuwa
amekosea. 12 Kabla ya watu kadhaa kuja kutoka kwa Yakobo, Kefa alikuwa akila
pamoja na watu wa mataifa. Lakini hawa watu walipokuja, aliacha na kuondoka
kutoka kwa watu wa mataifa. Alikuwa anaogopa watu ambao walihitaji tohara.
13 Vilevile Wayahudi wengine waliungana na unafiki huu pamoja na Kefa. Matokeo
yake yalikuwa kwamba hata Barnaba alichukuliwa na unafiki wao. 14 Lakini
nilipoona kwamba walikuwa hawafuati injili ya kweli, nilimwambia Kefa mbele yao
wote, "Kama ninyi ni Wayahudi lakini mnaishi tabia za watu wa mataifa badala
ya tabia za Kiyahudi, kwa nini mnawalazimisha watu wa mataifa kuishi kama
Wayahudi?" 15 Sisi ambao ni Wayahudi kwa kuzaliwa na siyo "Watu wa mataifa
wenye dhambi " 16 fahamu kwamba hakuna anayehesabiwa haki kwa matendo ya
sheria. Badala yake, wanahesabiwa haki kwa imani ndani ya Yesu Kristo. Tulikuja
kwa imani ndani ya Kristo Yesu ili kwamba tunahesabiwa haki kwa imani ndani ya
Kristo na siyo kwa matendo ya sheria. Kwa matendo ya sheria hakuna mwili utakao
hesabiwa haki. 17 Lakini kama tunapomtafuta Mungu kwa kutuhesabia haki ndani
ya Kristo, tunajikuta wenyewe pia kuwa wenye dhambi, je Kristo alifanywa mtumwa
wa dhambi? Siyo hivyo! 18 Maana kama nikijenga tegemeo langu juu ya kutunza
sheria, tegemeo ambalo nilikwisha liondoa, najionesha mwenyewe kuwa mvunja
sheria. 19 Kupitia sheria nilikufa kwa sheria, kwa hiyo napaswa kuishi kwa ajili
ya Mungu. 20 Nimesulubiwa pamoja na Kristo. Si mimi tena ninayeishi, bali Kristo
anaishi ndani yangu. Maisha ninayoishi katika mwili ninaishi kwa imani ndani ya
Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda na akajitoa kwa ajili yangu. 21 Siikani neema
ya Mungu, maana kama haki ilikuwepo kupitia sheria, basi Kristo angekuwa amekufa
bure.

# 3

1 Wagalatia wajinga, ni jicho gani ovu lililowaharibu? Je Yesu Kristo hakuoneshwa
kama msulubiwa mbele ya macho yenu? 2 Mimi nataka tu kufahamu hili kutoka
kwenu. Je mlimpokea Roho kwa matendo ya sheria au kwa kuamini kile mlichosikia?
3 Je, ninyi ni wajinga kiasi hiki? Je mlianza katika Roho ili mmalize katika mwili? 4 Je
mliteseka kwa mambo mengi bure, kama kweli yalikuwa ya bure? 5 Je yeye atoaye
Roho kwenu na kutenda matendo ya nguvu kati yenu hufanya kwa matendo ya sheria
au kwa kusikia pamoja na imani? 6 Abraham "Alimwamini Mungu akahesabiwa
kuwa mwenye haki". 7 Kwa namna ile ile eleweni kwamba, wale ambao wanaamini
ni watoto wa Abrahamu. 8 Andiko lilitabiri kwamba Mungu angewahesabia haki
watu wa mataifa kwa njia ya imani. Injili ilihubiriwa kwanza kwa Abrahamu: "katika
wewe mataifa yote yatabarikiwa". 9 Ili baadaye wale ambao wana imani wabarikiwe
pamoja na Abrahamu, ambaye alikuwa na imani. 10 Wale ambao wanategemea
matendo ya sheria wako chini ya laana. Kwa kuwa imeandikwa, "Amelaaniwa kila
mtu ambaye hashikamani na mambo yote yaliyoandikwa katika kitabu cha sheria,

kuyatenda yote.” 11 Sasa ni wazi kwamba Mungu hamhesabii haki hata mmoja
kwa sheria, kwa kuwa “Mwenye haki ataishi kwa imani”. 12 Sheria haitokani na
imani, lakini badala yake “Ambaye hufanya mambo haya katika sheria, ataishi kwa
sheria.” 13 Kristo alitukomboa sisi kutoka katika laana ya sheria wakati alipofanyika
laana kwa ajili yetu. Kwa kuwa imeandikwa, “Amelaaniwa kila mtu aangikwaye
juu ya mti.” 14 Lengo lilikuwa kwamba, baraka ambazo zilikuwa kwa Ibrahimu
zingekuja kwa watu wa mataifa katika Kristo Yesu, ili kwamba tuweze kupokea ahadi
ya Roho kupitia imani. 15 Ndugu, ninazungumza kwa namna ya kibinadamu. Hata
wakati ambapo agano la kibinadamu limekwisha kuwekwa imara, hakuna awezaye
kupuuza au kuongezea. 16 Sasa ahadi zilisemwa kwa Ibrahim na kwa kizazi chake.
Haisemi, “kwa vizazi,” kumaanisha wengi, bali badala yake kwa mmoja pekee, “kwa
kizazi chako,” ambaye ni Kristo. 17 Sasa nasema hivi, sheria ambayo ilikuja miaka
430 baadaye, haiondoi agano la nyuma lililowekwa na Mungu. 18 Kwa kuwa kama
urithi ungelikuja kwa njia ya sheria, usingekuwa tena umekuja kwa njia ya ahadi.
Lakini Mungu aliutoa bure kwa Ibrahimu kwa njia ya ahadi. 19 Kwa nini sasa sheria
ilitolewa? Iliongezwa kwa sababu ya makosa, mpaka mzao wa Ibrahimu aje kwa
wale ambao kwao alikuwa ameahidiwa. Sheria iliwekwa katika shinikizo kupitia
malaika kwa mkono wa mpatanishi. 20 Sasa mpatanishi humaanisha zaidi ya mtu
mmoja, bali Mungu ni mmoja peke yake. 21 Kwa hiyo je sheria iko kinyume na
ahadi za Mungu? La hasha! Kwa kuwa kama sheria iliyokuwa imetolewa ilikuwa
na uwezo wa kuleta uzima, haki ingepatikana kwa sheria. 22 Lakini badala yake,
andiko limefunga mambo yote chini ya dhambi. Mungu alifanya hivi ili kwamba
ahadi yake ya kutuokoa sisi kwa imani katika Yesu Kristo iweze kupatikana kwa wale
wanao amini. 23 Lakini kabla ya imani katika Kristo haijaja, tulikuwa tumefungwa
na kuwa chini ya sheria hadi uje ufunuo wa imani. 24 Kwa hiyo sheria ilifanyika
kiongozi wetu hadi Kristo alipokuja, ili kwamba tuhesabiwe haki kwa imani. 25 Sasa
kwa kuwa imani imekuja, hatuko tena chini ya mwangalizi. 26 Kwa kuwa ninyi nyote
ni watoto wa Mungu kupitia imani katika Kristo Yesu. 27 Wote ambao mlibatizwa
katika Kristo mmejivika Kristo. 28 Hakuna Myahudi wala Myunani, mtumwa wala
huru, mwanaume wala mwanamke, kwa kuwa ninyi nyote ni mmoja katika Kristo
Yesu. 29 Kama ninyi ni wa Kristo, basi ni uzao wa Ibrahimu, warithi kwa mujibu wa
ahadi.

# 4

1 Ninasema kwamba maadamu mrithi ni mtoto, hana tofauti na mtumwa, hata in-
gawa ni mmiliki wa mali yote. 2 Badala yake, yuko chini ya waangalizi na wadhamini
mpaka wakati uliowekwa na baba yake. 3 Kadhalika pia na sisi, tulipokuwa watoto,
tulishikiliwa katika utumwa wa kanuni za kwanza za ulimwengu. 4 Lakini wakati
sahihi ulipofika, Mungu alimtuma mwanawe, mzaliwa wa mwanamke, mzaliwa chini
ya sheria. 5 Alifanya hivi ili kuwakomboa wale waliokuwa chini ya sheria, ili kwamba
tupokee hali ya kuwa kama wana. 6 Kwa sababu ninyi ni wana, Mungu alimtuma
Roho wa mwanawe ndani ya mioyo yetu, Roho aitaye, “Abba, Baba.” 7 Kwa sababu
hii wewe si mtumwa tena bali mwana. Kama ni mwana, basi wewe pia ni mrithi
kupitia Mungu. 8 Hata kabla, wakati hamkumjua Mungu, mlikuwa watumwa kwa
wale ambao kwa asili si miungu kabisa. 9 Lakini sasa kwamba mnamjua Mungu, au
kwamba mnajulikana na Mungu, kwa nini mnarudi tena kwenye kanuni dhaifu za
kwanza na zisizo za thamani? Je mnataka kuwa watumwa tena? 10 Mnashika kwa
uangalifu siku maalumu, miandamo ya miezi, majira, na miaka. Ninaogopa kwa ajili
yenu. 11 Ninaogopa kwamba kwa namna fulani nimejitaabisha bure. 12 Ninawasihi,
ndugu, muwe kama nilivyo, kwa kuwa pia nimekuwa kama mlivyo. Hamkunikosea.

13 Bali mnajua kwamba ilikuwa ni kwa sababu ya ugonjwa wa mwili kwamba
nilihubiri injili kwenu kwa mara ya kwanza. 14 Ingawa hali yangu ya mwili iliwaweka
katika jaribu, hamkunidharau au kunikataa. Badala yake mlinipokea kama malaika
wa Mungu, kana kwamba nilikuwa Kristo Yesu mwenyewe. 15 Kwa hiyo, iko wapi sasa
furaha yenu? kwa kuwa ninashuhudia kwenu kwamba, ikiwezekana, mungelin'goa
macho yenu na kunipa mimi. 16 Hivyo sasa, je nimekuwa adui yenu kwa sababu
ninawaambia ukweli? 17 Wanawatafuta kwa shauku, bali si kwa mema. Wanataka
kuwatenganisha ninyi na mimi ili muwafuate. 18 Ni vyema daima kuwa na shauku
kwa sababu zilizo njema, na si tu wakati ninapokuwa pamoja nanyi. 19 Wanangu
wadogo, ninaumwa uchungu kwa ajili yenu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu.
20 Ningependa kuwepo pale pamoja nanyi sasa na kugeuza sauti yangu, kwa sababu
ninamashaka juu yenu. 21 Niambieni, ninyi ambao mnatamani kuwa chini ya sheria,
hamsikii sheria isemavyo? 22 Kwa kuwa imeandikwa kwamba Abrahamu alikuwa
na wana wa kiume wawili, mmoja kwa yule mwanamke mtumwa na mwingine
kwa mwanamke huru. 23 Hata hivyo, yule wa mtumwa alizaliwa kwa mwili tu, bali
yule wa mwanamke huru alizaliwa kwa ahadi. 24 Mambo haya yanaweza kuelezwa
kwa kutumia mfano, kwa kuwa wanawake hawa wanafanana na maagano mawili.
Mojawapo kutoka katika mlima Sinai. Huzaa watoto ambao ni watumwa. huyu ni
Hajiri. 25 Sasa Hajiri ni mlima Sinai ulioko Arabuni. Hufananishwa na Yerusalem
ya sasa, kwa kuwa ni mtumwa pamoja na watoto wake. 26 Bali Yerusalemu ambayo
iko juu ni huru, na hii ndiyo mama yetu. 27 Kwa kuwa imeandikwa, “Furahi, wewe
mwanamke uliye tasa, wewe usiye zaa. Paza sauti na upige kelele kwa furaha, wewe
ambaye huna uzoefu wa kuzaa. kwa maana wengi ni watoto wa aliye tasa, zaidi ya
wale wa yule ambaye ana mume.” 28 Sasa ndugu, kama Isaka, ninyi ni watoto wa
ahadi. 29 Kwa wakati ule ambao mtu ambaye alizaliwa kwa mujibu wa mwili alimtesa
yule aliyezaliwa kwa mujibu wa Roho. Kwa sasa ni vilevile. 30 Maandiko husemaje?
“Muondoe mwanamke mtumwa pamoja na mwanawe wa kiume. Kwa kuwa mtoto
wa mwanamke mtumwa hatarithi pamoja na mtoto wa mwanamke huru.” 31 Kwa
hiyo, ndugu, sisi si watoto wa mwanamke mtumwa, bali ni wa mwanamke huru.

# 5

1 Ni kwa sababu Kristo alitupa uhuru ili tuwe huru. Hivyo, simameni imara wala
msinaswe tena katika kongwa la utumwa. 2 Tazama, Mimi Paulo, ninawaambia
kwamba ikiwa mtatahiriwa, Kristo hatawafaidia kwa njia yoyote ile. 3 Tena,
namshuhudia kila mwanaume aliyetahiriwa kwamba anapaswa kuwajibika kwa
sheria yote. 4 Mmetengwa mbali na Kristo, wale wote “mnaohesabiwa haki” kwa
sheria. Mmeanguka mbali na neema. 5 Maana kwa njia ya Roho, kwa imani
tunasubiri ujasiri wa haki. 6 Katika Kristo Yesu kutahiriwa au kutokutahiriwa hakuna
maana yoyote. Ni imani pekee inayofanya kazi kupitia upendo ndiyo humaanisha
kitu. 7 Mlikuwa mnapiga mbio vizuri. Nani aliwazuia kutokuitii kweli? 8 Ushawishi
wa kufanya hivyo hautoki kwake yeye anayewaita ninyi. 9 Chachu kidogo huathiri
donge zima. 10 Nina matumaini na ninyi katika Bwana kwamba hamtafikiri kwa
njia nyingine yoyote. Yeyote yule atakayewapotosha atabeba hukumu yake yeye
mwenyewe, yeyote yule. 11 Ndugu, kama naendelea kutangaza tohara, kwanini
bado ninateswa? Kwa suala hilo kile ambacho ni kizuizi cha msalaba kitaweza
kuharibiwa. 12 Ni matakwa yangu kuwa wale wanaowaongoza vibaya watajihasi
wenyewe. 13 Mungu amewaiteni ninyi, ndugu, kwenye uhuru. Ila msiutumie uhuru
wenu kama fursa kwa mwili. Badala yake kwa upendo mhudumiane ninyi kwa ninyi.
14 Kwa kuwa sheria yote imekamilika katika amri moja; nayo ni “Ni lazima umpende
jirani yako kama wewe mwenyewe.” 15 Lakini kama mkiumana na kulana, jiangalieni

kwamba msijiharibu ninyi kwa ninyi. 16 Nasema, tembeeni kwa roho, na wala
hamtazitimiza tamaa za mwili. 17 Kwa kuwa mwili una tamaa kubwa dhidi ya Roho,
na Roho ina tamaa kubwa dhidi ya mwili. Hizi zinapingana kila moja na nyingine.
Matokeo ni kwamba hamfanyi vitu mnavyotamani kuvifanya. 18 Lakini kama Roho
anawaongoza ninyi, hamko chini ya sheria. 19 Sasa matendo ya mwili yanaonekana.
Nayo ni uasherati, uchafu, ufisadi, 20 ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi,
husuda, kuwaka hasira, ushindani, faraka, mgawanyiko wa madhehebu, 21 wivu,
ulevi, ulafi na mambo mengine kama haya. Nawaonya ninyi, kama nilivyowaonya
mwanzoni, kwamba wale wanaofanya mambo kama hayo hawataurithi ufalme wa
Mungu. 22 Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, ukarimu,
utu wema, imani, 23 upole, na kiasi. Hakuna sheria dhidi ya mambo kama hayo.
24 Wale walio wa Kristo Yesu wameusulubisha mwili pamoja na shauku na tamaa zao
mbaya. 25 Kama tukiishi kwa Roho, pia tutembee kwa Roho. 26 Tusiwe wa kujivuna,
tusichokozane kila mmoja na mwenzake, wala tusioneane wivu.

# 6

1 Ndugu, ikiwa mtu amekamatwa katika uovu, ninyi mlio wa kiroho, mnawiwa
kumrejesha huyo ndugu katika roho ya upole. Huku mkijiangalia wenyewe ili
msijaribiwe. 2 Mchukuliane mizigo, na kwa hiyo mtaikamilisha sheria ya Kristo.
3 Ikiwa mtu yeyote anajiona ni bora wakati si kitu, anajidanganya mwenyewe. 4 Kila
mmoja na aipime kazi yake. Kisha atakuwa na kitu mwenyewe peke yake cha
kujisifu, bila kujilinganisha mwenyewe na mtu yeyote. 5 Maana kila mtu atachukua
mzigo wake mwenyewe. 6 Mtu aliyefundishwa neno lazima amshirikishe mazuri
yote mwalimu wake. 7 Msidanganyike. Mungu hadhihakiwi. Kila apandacho mtu,
ndicho atakachovuna pia. 8 Kila apandaye mbegu katika asili yake ya dhambi
atavuna uharibifu, lakini yeye apandaye mbegu katika Roho, atavuna uzima wa
milele kutoka kwa Roho. 9 Tusichoke katika kutenda mema, maana kwa wakati
wake tutavuna ikiwa hatutakata tamaa. 10 Hivyo basi, wakati tutakapokuwa na
nafasi, tutende mema kwa kila mmoja. Tutende mema zaidi hasa kwa walio
ndani ya imani. 11 Angalieni ukubwa wa barua nilizowaandikia kwa mkono wangu
mwenyewe. 12 Wale wanaotaka kufanya mema kwa mtazamo wa mwili ndiyo wenye
kuwalazimisha mtahiriwe. Wanafanya hivyo kwa sababu wasiingie kwenye mateso
ya msalaba wa Kristo. 13 Maana hata hao waliotahiriwa wenyewe hawaishiki sheria.
Badala yake wanataka ninyi mtahiriwe ili waweze kujivunia miili yenu. 14 Isitokee
nikajivuna isipokuwa kwa msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo. Ni katika yeye
ulimwengu umesulubiwa kwangu na mimi katika ulimwengu. 15 Kwa kuwa haijalishi
kutahiriwa au kutokutahiriwa kuwa ni kitu. Badala yake uzao mpya ni muhimu.
16 Kwa wote wenye kuishi kwa kanuni hii, wawe na amani na rehema iwe juu yao
wote, na juu ya Israel ya Mungu. 17 Tangu sasa mtu yeyote asinitaabishe, maana
nimebeba chapa za Yesu mwilini mwangu. 18 Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo iwe
na roho zenu, ndugu. Amina.

# Waefeso

1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu, kwa waliotengwa kwa ajili
ya Mungu walioko Efeso na ambao ni waaminifu katika Kristo Yesu. 2 Neema iwe
kwenu na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu na Bwana Yesu Kristo. 3 Mungu na
Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo apewe sifa. Ni yeye aliyetubariki kwa kila baraka za
kiroho, katika mahali pa mbingu ndani ya Kristo. 4 Kabla ya kuumbwa ulimwengu,
Mungu alituchagua sisi ambao tunaamini katika Kristo. Alituchagua sisi ili tuweze
kuwa watakatifu na tusiolaumika mbele yake. 5 Katika pendo Mungu alituchagua
mwanzo kwa kututwaa kama watoto wake kwa njia ya Yesu Kristo. Alifanya hivi kwa
sababu alipendezwa kufanya kile alichotamani. 6 Matokeo yake ni kwamba Mungu
anatukuzwa kwa neema ya utukufu wake. Hiki ndicho alichotupatia bure kwa
njia ya mpendwa wake. 7 Kwa kuwa katika mpendwa wake, tunaukombozi kupitia
damu yake, msamaha wa dhambi. Tunalo hili kwa sababu ya utajiri wa neema
yake. 8 Alifanya neema hii kuwa nyingi kwa ajili yetu katika hekima na ufahamu.
9 Mungu alifanya ijulikane kwetu ile kweli iliyofichika ya mpango, kutokana na hamu
iliyodhihirishwa ndani ya Kristo. 10 Wakati nyakati zimetimia kwa utimilifu wa
mpango wake, Mungu ataviweka pamoja kila kitu cha mbinguni na cha juu ya nchi
ndani ya Kristo. 11 Katika Kristo tulikuwa tumechaguliwa na kukusudiwa kabla ya
wakati. Hii ilikuwa ni kutokana na mpango wa anayefanya vitu vyote kwa kusudi
la mapenzi yake. 12 Mungu alifanya hivyo ili kwamba tuweze kuwapo kwa sifa ya
utukufu wake. Tulikuwa wa kwanza kuwa na ujasiri ndani ya Kristo. 13 Ilikuwa
kwa njia ya Kristo kwamba mlisikia neno la kweli, injili ya wokovu wenu kwa njia
ya Kristo. Ilikuwa katika yeye pia kwamba mmeamini na kutiwa mhuri na Roho
Mtakatifu aliye ahidiwa. 14 Roho ndiyo dhamana ya urithi wetu mpaka umiliki
utakapopatikana. Hii ilikuwa ni kwa sifa ya utukufu wake. 15 Kwa sababu hii, tangu
wakati niliposikia kuhusu imani yenu ndani ya Bwana Yesu na kuhusu pendo lenu
kwa wale wote ambao wametengwa kwa ajili yake. 16 Sijaacha kumshukuru Mungu
kwa ajili yenu na kuwataja katika maombi yangu. 17 Ninaomba kwamba Mungu wa
Bwana wetu Yesu Kristo, baba wa utukufu, atawapeni roho ya hekima, mafunuo ya
ufahamu wake. 18 Ninaomba kwamba macho yenu ya moyoni yatiwe nuru kwa ninyi
kujua ni upi ujasiri wa kuitwa kwenu. Naomba kwamba mjue utajiri wa utukufu wa
urithi wake miongoni mwa wale waliotengwa kwa ajili yake. 19 Naomba kwamba
ujue ukuu uzidio wa nguvu yake ndani yetu ambao tunaamini. Huu ukuu ni kutokana
na kufanya kazi katika nguvu zake. 20 Hii ni nguvu iliyofanya kazi ndani ya Kristo
wakati Mungu alipomfufua kutoka kwa wafu na kumketisha katika mkono wake
wa kuume katika mahali pa mbingu. 21 Alimketisha Kristo juu mbali na utawala,
mamlaka, nguvu, enzi, na kila jina litajwalo. Alimketisha Yesu si tu kwa wakati huu
lakini kwa wakati ujao pia. 22 Mungu amevitiisha vitu vyote chini ya miguu ya Kristo.
Amemfanya yeye kichwa juu ya vitu vyote katika kanisa. 23 Ni kanisa kwamba ndilo
mwili wake, ukamilifu wake ambaye hujaza vitu vyote katika njia zote.

## 2

1 Kama vile mlivyo kuwa mmekufa katika makosa na dhambi zenu. 2 Ilikuwa
katika haya kwamba kwanza mlienenda kulingana na nyakati za ulimwengu huu.
Mlikuwa mkienenda kwa kufuata mtawala wa mamlaka ya anga. Hii ndiyo roho
yake yule afanyaye kazi katika wana wa kuasi. 3 Sisi wote hapo mwanzo tulikuwa
miongoni mwa hawa wasioamini. Tulikuwa tukitenda kwa namna ya tamaa mbaya

za miili yetu. Tulikuwa tukifanya mapenzi ya mwili na ufahamu wetu. Tulikuwa
kwa asili wana wa ghadhabu kama wengine. 4 Lakini Mungu ni mwingi wa rehema
kwa sababu ya pendo lake kubwa alilotupenda sisi. 5 Wakati tulipokuwa wafu katika
makosa yetu, alituleta pamoja katika maisha mapya ndani ya Kristo. Ni kwa neema
kwamba mmeokolewa. 6 Mungu alitufufua pamoja na kutufanya kukaa pamoja
katika mahali pa mbingu ndani ya Kristo Yesu. 7 Alifanya hivi ili katika nyakati
zijazo aweze kutuonesha utajiri mkuu wa neema yake. Hutuonesha sisi hili kwa
njia ya wema wake ndani ya Kristo Yesu. 8 Kwa neema mmeokolewa kwa njia ya
imani. Na hii haikutoka kwetu. Ni zawadi ya Mungu. 9 Haitokani na matendo.
Matokeo yake, asiwepo mmoja wapo wa kujisifu. 10 Kwa sababu sisi tu kazi ya
Mungu, tumeumbwa katika Kristo Yesu kutenda matendo mema. Ni matendo haya
ambayo Mungu aliyapanga tangu zamani za kale kwa ajili yetu, ili tutembee katika
hayo. 11 Kwa hiyo kumbukeni kwamba hapo zamani mlikuwa watu wa Mataifa kwa
jinsi ya mwili. Mnaitwa “msio na tohara” kwa kile kinachoitwa tohara ya mwili
inayofanywa kwa mikono ya binadamu. 12 Kwa wakati huo mlikuwa mmetengwa na
Kristo. Mlikuwa wageni kwa watu wa Israel. Mlikuwa wageni kwa agano la ahadi.
Hamkuwa na uhakika wa wakati ujao. Mlikuwa bila Mungu katika ulimwengiu.
13 Lakini sasa katika Kristo Yesu ninyi ambao hapo mwanzo mlikuwa mbali na Mungu
mmeletwa karibu na Mungu kwa damu ya Kristo. 14 Kwa maana yeye ndiye amani
yetu. Alifanya wawili kuwa mmoja. Kwa mwili wake aliuharibu ukuta wa utengano
ambao ulikuwa umetutenganisha, huo uadui. 15 Kwamba alikomesha sheria ya
amri na kanuni ili kwamba aumbe mtu mmoja mpya ndani yake. Akafanya amani.
16 Alifanya hivi ili kuwapatanisha makundi mawili ya watu kuwa mwili mmoja kwa
Mungu kupitia msalaba. Kwa njia ya msalaba aliufisha uadui. 17 Yesu alikuja na
kutangaza amani kwenu ninyi mliokuwa mbali na amani kwao wale waliokuwa
karibu. 18 Kwa maana kwa njia ya Yesu sisi wote wawili tuna nafasi kwa yule
Roho mmoja kuingia kwa Baba. 19 Hivyo basi, ninyi watu wa mataifa si wasafiri
na wageni tena. Bali ni wenyeji pamoja na wale waliotengwa kwa ajili ya Mungu
na wajumbe katika nyumba ya Mungu. 20 Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na
manabii. Kristo Yesu mwenyewe alikuwa jiwe kuu la pembeni. 21 Katika yeye jengo
lote limeungamanishwa pamoja na kukua kama hekalu ndani ya Bwana. 22 Ni ndani
yake ninyi nanyi mnajengwa pamoja kama mahali pa kuishi pa Mungu katika Roho.

# 3

1 Kwa sababu ya hii mimi, Paulo, ni mfungwa wa Yesu Kristo kwa ajili yenu
Mataifa. 2 Na amini ya kwamba mmesikia juu ya kazi ya neema ya Mungu aliyo
nipa kwa ajili yenu. 3 Nawaandikieni kutokana na jinsi ufunuo ulivyo funuliwa
kwangu. Huu ni ukweli uliyofichika ambao niliandika kwa kifupi kwenye barua
nyingine. 4 Usomapo kuhusu haya, utaweza kutambua busara yangu katika ukweli
huu uliofichika kuhusu Kristo. 5 Kwa vizazi vingine ukweli huu haukufanywa
utambulike kwa wana wa watu. Ila kwa sasa umewekwa wazi kwa Roho kwa Mitume
waliotengwa na Manabii. 6 Ukweli huu uliofichika ni kwamba watu wa Mataifa ni
washiriki wenzetu na wajumbe wenzetu wa mwili. Niwashiriki pamoja na ahadi ya
Kristo Yesu kupitia injili. 7 Na kwa hili nimefanyika mtumishi kwa zawadi ya neema
ya Mungu iliyotolewa kwangu kupitia utendaji wa nguvu yake. 8 Mungu alitoa zawadi
hii kwangu, japo kuwa mimi ni mtu mdogo wa wote katika wale waliotengwa kwa
ajili ya Mungu. Zawadi hii ni kwamba inanipasa kuwatangazia mataifa injili yenye
utajiri usiochunguzika wa Kristo. 9 inanipasa kuwaangazia watu wote juu ya nini ni
mpango wa Mungu wa siri. Huu ni mpango ambao ulikuwa umefichwa kwa miaka
mingi iliyopita, na Mungu ambaye aliviumba vitu vyote. 10 Hii ilikuwa kwamba,

kupitia Kanisa, watawala na mamlaka katika sehemu za mbingu wapate kujua pande
nyingi za asili ya hekima ya Mungu. 11 Haya yangetokea kupitia mpango wa milele
ambao aliukamilisha ndani ya Kristo Yesu Bwana wetu. 12 Kwa kuwa katika Kristo
tuna ujasiri na uwezo wa kuingia kwa ujasiri kwa sababu ya imani yetu kwake.
13 Kwa hiyo nawaomba msikate tamaa kwasababu ya mateso yangu kwa ajili yenu.
Haya ni utukufu wenu. 14 Kwa sababu hii napiga magoti kwa Baba. 15 ambaye
kwa yeye kila familia mbinguni na juu ya nchi imeitwa jina. 16 Ninaomba kwamba
apate kuwanemesha, kutokana na utajiri wa utukufu wake, awafanye imara kwa
nguvu kupitia Roho wake, ambaye yu ndani yenu. 17 Ninaomba kwamba Kristo aishi
ndani ya mioyo yenu kupitia imani. 18 Ninaomba kwamba muwe na shina na msingi
wa upendo wake. Muwe katika pendo lake ili muweze kuelewa, pamoja na wote
waaminio, jinsi upana, na urefu na kimo na kina cha upendo wa Kristo. 19 Ninaomba
Kwamba mjue ukuu wa upendo wa Kristo, ambao unazidi ufahamu. Mfanye haya ili
mjazwe na ukamilifu wote wa Mungu. 20 Na sasa kwake yeye awezaye kufanya kila
jambo, zaidi ya yote tuyaombayo au tuyawazayo, kupitia nguvu yake itendayo kazi
ndani yetu, 21 kwake yeye kuwe utukufu ndani ya kanisa na katika Kristo Yesu kwa
vizazi vyote milele na milele. Amina.

# 4

1 Kwa hiyo, kama mfungwa kwa ajili ya Bwana, nawasihi mtembee sawasawa
na wito ambao Mungu aliwaita. 2 Muishi kwa unyenyekevu mkuu na upole na
uvumilivu. Mkichukuliana katika upendo. 3 Fanyeni bidii kuutunza umoja wa Roho
katika kifungo cha amani. 4 Kuna mwili mmoja na Roho moja, kama ambavyo pia
mlikuwa mmeitwa katika uhakika wa taraja moja la wito wenu. 5 Na kuna Bwana
mmoja, imani moja, ubatizo mmoja, 6 na Mungu mmoja na Baba wa wote. Yeye
yuko juu ya yote, na katika yote na ndani ya yote. 7 Kwa kila mmoja wetu amepewa
kipawa kulingana na kipimo cha kipawa cha Kristo. 8 Ni kama maandiko yasemavyo:
“Alipopaa juu sana, aliongoza mateka katika utumwa. Akatoa vipawa kwa watu.” 9 Ni
nini maana ya, “Alipaa,” isipokuwa kwamba alishuka pia pande za chini za dunia?
10 Yeye ambaye alishuka ni mtu yuleyule ambae pia alipaa mbali juu ya mbingu
zote. Alifanya hivi ili uwepo wake uwe katika vitu vyote. 11 Kristo alitoa vipawa
kama hivi: mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji, na waalimu. 12 Alifanya hivi
kuwawezesha waumini kwa ajili ya kazi ya huduma, kwa ajili ya kuujenga mwili wa
Kristo. 13 Anafanya hivi hadi sisi sote tufikie umoja wa imani na maarifa ya mwana
wa Mungu. Anafanya hivi hadi tuweze kukomaa kama wale waliofikia kimo kamili
cha Kristo. 14 Hii ni ili kwamba tusiwe tena kama watoto, tusirushwerushwe huku na
huko. Ili kwamba tusichukuliwe na kila aina ya upepo wa fundisho, kwa hila za watu
katika ujanja wa udanganyifu uliopotoka. 15 Badala yake, tutaongea ukweli katika
upendo na kukua zaidi katika njia zote ndani yake ambaye ndiye kichwa, Kristo.
16 Kristo ameunganisha, kwa pamoja, mwili wote wa waumini. Umeungamanishwa
pamoja na kila kiungo ili kwamba mwili wote ukue na kujijenga wenyewe katika
upendo. 17 Kwa hiyo, nasema hili, na nawasihi katika Bwana: Msitembee tena kama
watu wa mataifa wanavyotembea katika ubatili wa akili zao. 18 Wametiwa giza
katika mawazo yao. Wamefukuzwa kutoka katika uzima wa Mungu kwa ujinga ulio
ndani yao kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao. 19 Hawajisikii aibu. Wamejikabidhi
wenyewe kwa ufisadi katika matendo machafu, katika kila aina ya uchoyo. 20 Lakini,
hivi sivyo mlivyojifunza kuhusu Kristo. 21 Nadhani kwamba mmesikia kuhusu yeye.
Nadhani kwamba mmekuwa mkifundishwa katika yeye, kama tu ukweli ulivyo ndani
ya Yesu. 22 Lazima mvue mambo yote yanayoendana na mwenendo wenu wa zamani,
utu wa zamani. Ni utu wa zamani unaooza kwa sababu ya tamaa za udanganyifu.

23 Vueni utu wenu wa zamani ili kwamba mfanywe upya katika roho ya akili zenu.
24 Fanyeni hivi ili muweze kuvaa utu mpya, unaoendana na Mungu. Umeumbwa
katika haki na utakatifu wa kweli. 25 Kwa hiyo, weka mbali udanganyifu. "Ongeeni
ukweli, kila mmoja na jirani yake," kwa sababu tu washirika kwa kila mmoja kwa
mwenzake. 26 Mwe na hasira, lakini msitende dhambi." Jua lisizame mkiwa katika
hasira zenu. 27 Msimpe Ibilisi nafasi. 28 Yeyote aibaye lazima asiibe tena. Badala yake
ni lazima afanye kazi. Afanye kazi yenye manufaa kwa mikono yake, ili kwamba
aweze kumhudumia mtu aliye na hitaji. 29 Kauli mbaya isitoke kinywani mwenu.
Badala yake, maneno lazima yatoke katika vinywa vyenu yafaayo kwa mahitaji,
kuwapa faida wale wanaosikiliza. 30 Na msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu.
Ni kwa Yeye kwamba mmewekewa muhuri kwa ajili ya siku ya ukombozi. 31 Lazima
muweke mbali uchungu wote, ghadhabu, hasira, ugomvi, na matusi, pamoja na kila
aina ya uovu. Iweni wema ninyi kwa ninyi. 32 Mwe na huruma. Msameheane ninyi
kwa ninyi, kama vile Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.

# 5

1 Kwa hiyo muwe watu wa kumfuata Mungu, kama watoto wake wapendwao.
2 Mtembee katika pendo, vilevile kama Kristo alivyotupenda sisi, alijitoa mwenyewe
kwa ajili yetu. Yeye alikuwa sadaka na dhabihu, kuwa harufu nzuri ya kumfurahisha
Mungu. 3 Zinaa au uchafu wowote na tamaa mbaya lazima visitajwe kati yenu,
kama inavyotakiwa kwa waaminio, 4 wala machukizo yasitajwe, mazungumzo ya
kipumbavu, au mizaha ya udhalilishaji, ambayo siyo sawa, badala yake iwepo
shukrani. 5 Mnaweza kuwa na uhakika ya kwamba kuna zinaa, uchafu, wala
atamaniye, huyo nimwabudu sanamu, hana urithi wowote katika ufalme wa Kristo
na Mungu. 6 Mtu yote asikudanganye kwa maneno matupu, kwa sababu ya mambo
haya hasira ya Mungu inakuja juu ya wana wasiotii. 7 Hivyo usishiriki pamoja nao.
8 Kwa kuwa ninyi mwanzo mlikuwa giza, lakini sasa mmekuwa nuru katika Bwana.
Hivyo tembeeni kama watoto wa nuru. 9 Kwa kuwa matunda ya nuru yanajumuisha
uzuri wote, haki na ukweli. 10 Tafuta kile kinacho furahisha kwa Bwana. 11 Usiwepo
ushiriki katika kazi za giza zisizo na matunda, badala yake ziweke wazi. 12 Kwa
sababu mambo yanayofanywa na wao sirini ni aibu sana hata kuyaelezea. 13 Mambo
yote, yanapofichuliwa na nuru, huwa wazi, 14 kwa kuwa Kila kitu kilichofichuliwa
kinakuwa nuruni. Hivyo husema hivi, "Amka, wewe uliyelala, na inuka kutoka wafu
na Kristo atang'aa juu yako." 15 Hivyo iweni makini jinsi mtembeavyo, siyo kama
watu wasio werevu bali kama werevu. 16 Ukomboeni muda kwa kuwa siku ni za
uovu. 17 Msiwe wajinga, badala yake, fahamuni nini mapenzi ya Bwana. 18 Msilewe
kwa mvinyo, huongoza kwenye uharibifu, badala yake mjazwe na Roho Mtakatifu.
19 Zungumzeni na kila mmoja wenu kwa zaburi, na sifa, na nyimbo za rohoni. Imbeni
na sifuni kwa moyo kwa Bwana. 20 Daima toa shukrani kwa mambo yote katika
jina la Kristo Yesu Bwana wetu kwa Mungu Baba. 21 Jitoeni wenyewe kila mmoja
kwa mwingine kwa heshima ya Kristo. 22 Wake, jitoeni kwa waume zenu, kama
kwa Bwana. 23 Kwa sababu mume ni kichwa cha mke, kama Kristo alivyo kichwa
cha kanisa. Ni mwokozi wa mwili. 24 Lakini kama kanisa lilivyo chini ya Kristo,
vilevile wake lazima wafanye hivyo kwa waume zao katika kila jambo. 25 Waume,
wapendeni wake zenu kama vile Kristo alivyolipenda kanisa na akajitoa mwenyewe
kwa ajili yake. 26 Alifanya hivyo ili liwe takatifu. Alilitakasa kwa kuliosha na maji
katika neno. 27 Alifanya hivi ili kwamba aweze kujiwasilishia mwenyewe kanisa
tukufu, pasipo na doa wala waa au kitu kifananacho na haya, badala yake ni takatifu
lisilo na kosa. 28 Kwa njia ile ile, waume wanatakiwa kuwapenda wake zao kama
miili yao. Yule ampendae mke wake anajipenda mwenyewe. 29 Hakuna hata mmoja

anayechukia mwili wake. Badala yake, huurutubisha na kuupenda, kama Kristo pia
alivyolipenda kanisa. 30 Kwa kuwa sisi ni washiriki wa mwili wake. 31 “Kwa sababu
hii mwanaume atamwacha baba yake na mama yake na ataungana na mke wake, na
hao wawili watakuwa mwili mmoja”. 32 huu ulikuwa umefichika. Lakini ninasema
kuhusu Kristo na kanisa. 33 Walakini, kila mmoja wenu lazima ampende mke wake
kama mwenyewe, na mke lazima amheshimu mumewe.

# 6

1 Watoto watiini wazazi wenu katika Bwana, kwa maana hii ni haki. 2 “Mheshimu
baba yako na mama yako” (Maana hii ndiyo amri ya kwanza yenye ahadi), 3 “ili
iwe heri kwenu na muweze kuishi maisha marefu juu ya nchi.” 4 Na ninyi akina
baba, msiwakwaze watoto na kuwasababishia hasira, badala yake, waleeni katika
maonyo na maagizo ya Bwana. 5 Enyi watumwa, iweni watiifu kwa mabwana zenu
wa hapa duniani kwa heshima kubwa na kutetemeka kwa hofu itokayo mioyoni
mwenu. muwe watiifu kwao kama vile mnavyomtii Kristo. 6 Utii wenu usiwe tu
pale mabwana zenu wanapowatazama ili kuwafurahisha. Badala yake, iweni watiifu
kama watumwa wa Kristo. Fanyeni Mapenzi ya Mungu kutoka mioyoni mwenu,
7 watumikieni kwa mioyo yenu yote, kwa kuwa mnamtumikia Bwana na wala si
wanadamu, 8 mnapaswa kujua kwamba katika kila tendo jema mtu analofanya,
atapokea zawadi kutoka kwa Bwana, ikiwa ni mtumwa au mtu huru. 9 Na ninyi
mabwana fanyeni vivyo hivyo kwa watumwa wenu. Msiwatishe mkijua kwamba
yeye aliye Bwana wa wote ni yule aliye mbinguni. Mkijua kuwa hakuna upendeleo
ndani yake. 10 Hatimaye, iweni na nguvu katika Bwana na katika uwezo wa nguvu
zake. 11 Vaeni silaha zote za Mungu, ili kwamba mpate kusimama kinyume na
hila za shetani. 12 kwa kuwa vita yetu si ya damu na nyama, bali ni dhidi ya
falme na mamlaka ya roho na watawala wa ulimwengu wa uovu na giza, dhidi
ya pepo katika sehemu za mbingu. 13 Kwa hiyo, vaeni silaha zote za Mungu, ili
mpate kusimama imara dhidi ya uovu katika kipindi hiki kiovu. Baada ya kumaliza
kila kitu, mtasimama imara. 14 Hatimaye simameni imara. Fanyeni hivi baada
ya kuwa mmefunga mkanda katika kweli na haki kifuani. 15 Fanyini hivi mkiwa
mmevaa utayari miguuni mwenu wa kutangaza injili ya amani. 16 Katika kila hali
mkichukua ngao ya imani, ambayo itakuwezesha kuizima mishale ya yule mwovu.
17 Vaeni kofia ya wokovu na upanga wa Roho, ambayo ni neno la Mungu. 18 pamoja
na maombi na dua. Ombeni kwa Roho kila wakati. Kwa mtazamo huu iweni
waangalifu kila wakati kwa uvumilivu wote na maombi kwa ajili ya waamini wote.
19 Ombeni kwa ajili yangu, ili nipewe ujumbe ninapofungua mdomo wangu. Ombeni
kwamba nieleweshe kwa ujasiri kweli iliyofichika ihusuyo injili. 20 Ni kwa ajili ya
injili mimi ni balozi niliyefungwa minyororo, ili kwamba ndani mwao niseme kwa
ujasiri kama ninavyowiwa kusema. 21 Lakini ninyi pia mjue mambo yangu na jinsi
ninavyoendelea, Tikiko ndugu yangu kipenzi na mtumishi mwaminifu katika Bwana,
atawajulisha kila kitu. 22 Nimemtuma kwenu kwa kusudi hili maalumu, ili kwamba
mjue mambo kuhusu sisi, aweze kuwafariji mioyo yenu. 23 Amani na iwe kwa ndugu,
na upendo pamoja na imani kutoka kwa Mungu baba na Bwana Yesu Kristo. 24 Neema
na iwe pamoja na wote wanampenda Bwana Yesu Kristo kwa pendo lile lisilo kufa.

# Wafilipi

[1] Paulo na Timotheo, watumishi wa Kristo Yesu, Kwa wale walitengwa katika Kristo
wanaoishi Filipi, pamoja na waangalizi na mashemasi. [2] Neema na iwe kwenu na
amani itokayo kwa Mungu Baba yetu na Bwana wetu Yesu Kristo. [3] Namshukuru
Mungu wangu kila ninapowakumbuka ninyi nyote. [4] Mara zote katika kila ombi
langu kwa ajili yenu ninyi nyote, huwa na furahi ninapowaombea. [5] Nina shukrani
nyingi kwa sababu ya ushirika wenu katika injili tangu siku ya kwanza mpaka leo.
[6] Nina hakika kuwa yeye aliyeanzisha kazi njema ndani yenu ataendelea kuikamilisha
mpaka siku ya Bwana Yesu Kristo. [7] Ni sawa kwangu kujisikia hivi juu yenu ninyi
nyote kwa sababu nimewaweka moyoni wangu. Maana ninyi mmekuwa washirika
wenza katika neema katika kifungo changu na katika utetezi na uthibitishaji wangu
wa injili. [8] Mungu ni shahidi wangu, jinsi nilivyo na shauku juu ya yenu nyote katika
undani wa pendo la Kristo Yesu. [9] Na ninaomba kwamba: upendo wenu uongezeke
zaidi na zaidi katika maarifa na ufahamu wote. [10] Ninaomba kwa ajili ya hili ili muwe
na uwezo wa kupima na kuchagua mambo yaliyo bora sana. Pia ninawaombea ili
muwe safi pasipokuwa na hatia yoyote katika siku ya Kristo. [11] Na pia ili mjazwe
na tunda la haki lipatikanalo katika Yesu Kristo, kwa utukufu na sifa ya Mungu.
[12] Sasa ndugu zangu, nataka mjue kuwa, mambo yaliyotokea kwangu yameifanya
injili iendelee sana. [13] Ndiyo maana vifungo vyangu katika Kristo, vimejulikana
kwa walinzi wa ikulu yote na kwa kila mtu pia. [14] Na ndugu wengi katika Bwana,
kwa sababu ya vifungo vyangu, wameshawishika na kuthubutu kulihubiri Neno
pasipo hofu. [15] Baadhi kweli hata humtangaza Kristo kwa fitina na ugomvi, na
pia wengine kwa nia njema. [16] Wale wanaomtangaza Kristo kwa upendo wanajua
kuwa nimewekwa hapa kwa ajili ya utetezi wa injili. [17] Bali wengine wanamtangaza
Kristo kwa ubinafsi na nia mbaya. Hudhani kuwa wanasababisha matatizo kwangu
katika minyororo yangu. [18] Kwa hiyo? Sijali, aidha njia ikiwa ni kwa hila au kwa
kweli, Kristo anatangazwa, na katika hili ninafurahia! Ndiyo, nitafurahia. [19] kwa
kuwa ninajua ya kuwa hili litaleta kufunguliwa kwangu. Jambo hili litatokea kwa
sababu ya maombi yenu na kwa msaada wa Roho wa Yesu Kristo. [20] Kulingana
na matarajio yangu ya uhakika na kweli ni kwamba, sitaona aibu. Badala yake,
kwa ujasiri wote, kama ambavyo siku zote na sasa, natarajia kuwa Kristo atainuliwa
katika mwili wangu, ikiwa katika uzima au katika kifo. [21] Kwa maana kwangu mimi,
kuishi ni Kristo na kufa ni faida. [22] Lakini, kama kuishi katika mwili huzaa tunda
katika kazi yangu, kwa hiyo sijui ni lipi la kuchagua. [23] Maana ninasukumwa sana
na mawazo haya mawili. Nina hamu ya kuuacha mwili na kuwa pamoja na Kristo,
kitu ambacho ni cha thamani sana sana. [24] Ingawa, kubaki katika mwili huu ni
jambo la muhimu sana kwa ajili yenu. [25] Kwa kuwa nina uhakika juu ya hili, ninajua
nitabaki na kuendelea kuwa pamoja nanyi nyote, kwa ajili ya maendeleo na furaha
ya imani yenu. [26] Na hii italeta furaha yenu kubwa katika Kristo Yesu, kwasababu
yangu itaongezeka, kwa sababu ya uwepo wangu tena pamoja nanyi. [27] Mnatakiwa
kuishi maisha yenu katika mwenendo mzuri uipasayo injili ya Kristo. fanyeni hivyo
ili nikija kuwaona au nisipokuja, nisikie kuwa mmesimama imara katika roho moja.
natamani kusikia kuwa mna roho moja, mkiishindania imani ya injili kwa pamoja.
[28] na msitishwe na kitu chochote kinachofanywa na maadui zenu. Hii kwao ni ishara
ya uharibifu. Bali kwenu ni ishara ya wokovu kutoka kwa Mungu. [29] kwa maana
ninyi mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, bali na kuteswa pia katika Yeye.

[30] kwa maana mna mgogoro uleule kama mliouona kwangu na mnasikia kwamba
ninao hata sasa.

# 2

[1] Ikiwa kuna kutiwa moyo katika Kristo. Ikiwa kuna faraja kutoka katika pendo
lake. Ikiwa kuna ushirika wa Roho. Ikiwa kuna rehema na huruma. [2] Ikamilisheni
furaha yangu kwa kunia mamoja mkiwa na upendo mmoja, mkiwa wamoja katika
roho, na kuwa na kusudi moja. [3] Msifanye kwa ubinafsi na majivuno. Isipokuwa
kwa unyenyekevu mkiwaona wengine kuwa bora zaidi yenu. [4] Kila mmoja wenu
asiangalie tu mahitaji yake binafsi, bali pia ajali mahitaji ya wengine. [5] Muwe na
nia kama aliyonayo Kristo Yesu. [6] Ingawaje yeye ni sawa na Mungu. Lakini hakujali
kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho. [7] Badala yake, alijishusha
mwenyewe. Alichukua umbo la mtumishi. Akajitokeza katika mfano wa wanadamu.
Alionekana mwanadamu. [8] Yeye alijinyeyekeza na kuwa mtii hadi kifo, kifo cha
msalaba. [9] Hivyo basi Mungu alimtukuza sana. Alimpa jina kuu lipitalo kila jina.
[10] Alifanya hivyo ili kwamba katika jina la Yesu kila goti sharti liiname. Magoti
ya walio mbinguni na walio juu ya ardhi na chini ya ardhi. [11] Na alifanya hivyo
ili kwamba kila ulimi sharti ukiri kwamba Yesu kristo ni Bwana, kwa utukufu wa
Mungu Baba. [12] Kwa hiyo basi, wapendwa wangu kama mnavyotii siku zote, Si tu
katika uwepo wangu lakini sasa ni zaidi sana hata pasipo uwepo wangu, uwajibikeni
wokovu wenu wenyewe kwa hofu na kutetemeka. [13] Kwa kuwa ni Mungu anayetenda
kazi ndani yenu ili kuwawezesha kunia na kutenda mambo yale yampendezayo yeye.
[14] Fanyeni mambo yote bila malalamiko na mabishano. [15] Fanyeni hivyo ili kwamba
msilaumike na kuwa watoto wa Mungu waaminifu wasiyo na lawama. Fanyeni
hivyo ili kwamba muwe nuru ya dunia, katika kizazi cha uasi na uovu. [16] Shikani
sana neno la uzima ili kwamba niwe na sababu ya kutukuza siku ya Kristo. Kisha
nitafahamu kwamba sikupiga mbio bure wala sikutaabika bure. [17] Lakini hata kama
ninamiminwa kama sadaka juu ya dhabidhu na huduma ya imani yenu, ninafurahi,
na ninafurahi pamoja nanyi nyote. [18] Vilevile na ninyi pia mnafurahi, na mnafurahi
pamoja nami. [19] Lakini natumaini katika Bwana Yesu kumtuma Timotheo kwenu hivi
karibuni, ili kwamba niweze kutiwa moyo nitakapojua mambo yenu. [20] Kwa kuwa
sina mwingine aliye na mtazamo kama wake, mwenye nia ya kweli kwa ajili yenu.
[21] Wengine wote ambao ningewatuma kwenu wanatafuta mambo yao binafsi tu, na
siyo mambo ya Yesu Kristo. [22] Lakini mnaijua thamani yake, kwa sababu kama mtoto
anavyomhudumia baba yake, ndivyo alivyotumika pamoja nami katika injili. [23] Kwa
hiyo ninatumaini kumtuma haraka pindi tu nitakapofahamu nini kitatokea kwangu.
[24] Lakini nina hakika katika Bwana kwamba mimi mwenyewe pia nitakuja hivi
karibuni. [25] Lakini nafikiri ni muhimu kumrejesha kwenu Epafradito. Yeye ni ndugu
yangu na mtenda kazi mwenzangu na askari mwenzangu, mjumbe na mtumishi
wenu kwa ajili ya mahitaji yangu. [26] Kwa sababu alikuwa na hofu na alitamani
kuwa pamoja nanyi nyote, kwa kuwa mlisikia kwamba alikuwa mgonjwa. [27] Maana
hakika alikuwa mgonjwa sana kiasi cha kufa. Lakini Mungu alimhurumia, na wema
huo haukuwa juu yake tu, lakini pia ulikuwa juu yangu, ili kwamba nisiwe na huzuni
juu ya huzuni. [28] Kwa hiyo ninamrejesha kweny haraka iwezekanavyo, Ili kwamba
mtakapomwona tena mpate kufurahi na mimi nitakuwa nimeondolewa wasi wasi.
[29] Mkaribisheni Epafradito katika Bwana kwa furaha zote. Waheshimuni watu kama
yeye. [30] Kwa kuwa ilikuwa kwa ajili ya kazi ya Kristo kwamba alikaribia kufa.
Alihatarisha maisha yake ili kuniokoa mimi na akafanya kile ambacho hamkuweza
kufanya katika kunihudumia mimi kwa mko mbali nami.

# 3

1 Hatimaye, ndugu zangu furahini katika Bwana. Sioni usumbufu kuwaandikia
tena maneno yaleyale. Haya mambo yatawapa usalama. 2 Jihadharini na mbwa.
Jihadharini na watenda kazi wabaya. Jihadharini na wale wajikatao miili yao. 3 Kwa
kuwa sisi nndiyo tohara. Sisi ndiyo huwa tumwabudu Mungu kwa msaada wa Roho.
Tujivuniao katika Kristo Yesu, na ambao hatuna ujasiri katika mwili. 4 Hata hivyo,
kama kungekuwa na mtu wa kuutumainia mwili huu, mimi ningeweza kufanya hivyo
zaidi. 5 Kwani nilitahiriwa siku ya nane, nilizaliwa katika kabila la Waisraeli. Ni wa
kabila la Benjamini. Ni Mwebrania wa waebrani. Katika kuitimiza haki ya sheria ya
Musa, nilikuwa, Farisayo. 6 Kwa juhudi zangu nililitesa Kanisa. Kwa tuitii haki ya
sheria, sikuwa na lawama kisheria. 7 Lakini katika mambo yote niliyoyaona kuwa ya
faida kwangu mimi, niliyahesabu kama takataka kwa sababu ya kumfahamu Kristo.
8 Kwa kweli, nayahesabu mambo yote kuwa hasara kutokana ubora wa kumjua wa
Kristo Yesu Bwana wangu. Kwa ajili yake nimeaacha mambo yote, nayahesabu
kama takataka ili nimpate Kristo 9 na nionekane ndani yake. Sina haki yangu
binafisi kutoka katika sheria, bali ninayo haki ile ipatikanayo kwa imani katika Kristo,
itokayo kwa Mungu, yenye msingi katika imani. 10 Sasa nataka kumfahamu yeye na
nguvu ya ufufuo wake na ushirika wa mateso yake. Nataka kubadilishwa na Kristo
katika mfano wa kifo chake, 11 angalau niweze kuwa na matumaini katika ufufuo
wa wafu. 12 Siyo kweli kwamba tayari nimeishayapata mambo hayo, au kwamba
nimekuwa mkamilifu katika hayo. Bali najitahidi ili niweze kupata kile kupata kile
nilichopatikana na Kristo Yesu. 13 Ndugu zangu, sidhani kwamba nimekwisha kupata
mambo haya. Bali nafanya jambo moja: nasahau ya nyuma nayatazamia ya mbele.
14 Najitahidi kufikia lengo kusudi ili nipate tuzo ya juu ya wito wa Mungu katika Kristo
Yesu. 15 Sote tulio ukulia wokovu, tunapaswa kuwaza namna hii. Na ikiwa mwingine
atafikiri kwa namna iliyotofauti kuhusu jambo lo lote, Mungu pia atalifunuao hiilo
kwenu. 16 Hata hivyo, hatua ifikia na tuenende katika mtindo huo. 17 Ndugu zangu,
niigeni mimi. Waangalieni kwa makini wale wanaoenenda kwa mfano ulio wa
jinsi yetu. 18 Wengi wanaoishi niwale ambao mara nyingi nimewaambieni, na sasa
nawaambia kwa machozi -wengi wanaishi kama maadui wa msalaba wa Kristo.
19 Mwisho wao ni uharibifu. Kwa kuwa Mungu wao ni tumbo, na kiburi chao kiko
katika aibu yao. Wanafikiria mambo ya kidunia. 20 Bali uraia wetu uko mbinguni,
ambako tunamtarajia mwokozi wetu Yesu Kristo. 21 Atabadilisha miili yetu dhaifu
kuwa kama mwili wake wa utukufu; kwa uweza ule ule unaomwezesha kuvidhibiti
vitu vyote.

# 4

1 Kwa hiyo wapendwa wangu, ambao nawatamani, ambao ni furaha na taji yangu.
Simameni imara katika Bwana, enyi rafiki wapendwa. 2 Ninakusihi wewe Eudia,
pia ninakusihi wewe Sintike, mrejeshe mahusiano ya amani kati yenu, kwa sababu
ninyi, nyote wawili mliungana na Bwana. 3 Kwa kweli, niwasihi pia ninyi watenda
kazi wenzangu, muwasaidie hawa wanawake kwa kuwa walitumika pamoja na mimi
katika kueneza injili ya Bwana tukiwa na Kelementi pamoja na watumishi wengine
wa Bwana, ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima. 4 katika Bwana
siku zote. tena nitasema, furahini. 5 Upole wenu na ujulikane kwa watu wote. Bwana
yuko karibu. 6 Msijisumbue kwa jambo lolote. Badala yake, fanyeni mambo yenu yote
kwa njia ya kusali, kuomba na kushukuru. Na mahitaji yenu yajulikane kwa Mungu.
7 Basi amani ya Bwana iliyo kuu kuliko ufahamu wote, italinda mioyo na mawazo
yenu kwa msaad Kristo Yesu. 8 Hatimaye, ndugu zangu; yatakafarini sana mambo
yote yenye ukweli, heshima, haki, usafi, upendo, na yale yenye taarifa njema, yenye

busara, pamoja na yale yanayohitaji kusifiwa. 9 Yatekelezeni mambo yale mliojifunza,
mliyopokea mliyoyasikia na yale mliyoyaona kwangu naye Baba yetu wa amani
atakuwa nanyi. 10 Ninayo furaha kubwa sana juu yenu katika Bwana kwa kuwa ninyi
mmeonyesha tena nia ya kujihusisha kwenu juu ya mahitaji yangu. Kwa kweli, hapo
awali mlitamani kunijali kwa mahitaji yangu japo hamkupata fursa ya kunisaidia.
11 Sisemi hivyo ili kujipatia kitu kwa ajili ya mahitaji yangu. Kwani nimejifunza
kuridhika katika hali zote. 12 Nafahamu kuishi katika hali ya kupungukiwa na pia
katika hali ya kuwa na vingi. Katika mazingira yote haya mimi nimejifunza siri
ya namna ya kula wakati wa shibe na jinsi ya kula wakati wa njaa, yaani vingi
na kuwa mhihtaji. 13 Ninaweza kufanya haya kwa kuwezeshwa na Yeye anitiaye
nguvu. 14 Hata hivyo, mlifanya vyema kushiriki nami katika dhiki zangu. 15 Ninyi
wafilipi mnafahamu kwamba mwanzo wa injili nilipoondoka Makedonia, hakuna
Kanisa lililoniwezesha katika mambo yanayohusu utoaji na kupokea isipokuwa ninyi
pekee yenu. 16 Hata nilipokuwa Thesaslonika, ninyi mlinitumia msaada zaidi ya
mara moja kwa ajili ya mahitaji yangu. 17 Simaanishi kwamba natafuta msaada. Bali
nasema ili mpate matunda yaletayo faida kwenu. 18 Nimepokea vitu vyote, na sasa
nimejazwa na vitu vingi. Nimepokea vitu vyenu kutoka kwa Epafradito. Ni vitu vizuri
vyenye kunukia mithiri ya manukato, vyenye kukubalika ambavyo vyote ni sadaka
inayompendeza Mungu. 19 Kwa ajili hiyo, Mungu wangu atawajazeni mahitaji yenu
kwa utajiri wa utukufu wake katikaYesu Kristo. 20 Sasa kwa Mungu na Baba yetu
uwe utukufu milele na milele. Amina. 21 Salamu zangu zimfikie kila muumini katika
Kristo Yesu. Wapendwa nilio nao hapa wanawasalimieni. 22 Pia waumini wote hapa
wanawasalimieni, hususani wale wa familia ya Kaisari. 23 Na sasa neema ya Bwana
wetu Yesu Kristo iwe na roho zenu.

# Wakolosai

1 Paulo, mtume wa Kristo Yesu kwa mapenzi ya Mungu, na Timotheo ndugu
yetu, 2 kwa waumini na ndugu waaminifu katika Kristo walioko Kolosai. Neema
iwe kwenu, na amani kutoka kwa Mungu Baba yetu. 3 Tunatoa shukrani kwa
Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, na tunawaombea mara kwa mara.
4 Tumesikia imani yenu katika Yesu Kristo na upendo mlionao kwa wale wote
waliotengwa kwa ajili ya Mungu. 5 Mna upendo huu kwa sababu ya taraja la
uhakika lililohifadhiwa mbinguni kwa ajili yenu. Mlisikia kuhusu taraja hiyo ya
uhakika kabla katika neno la kweli, injili, 6 ambayo imekuja kwenu. Injili hii
inazaa tunda na inaenea ulimwenguni kote. Imekuwa ikifanya hivi ndani yenu pia
tangu siku mlipoisikia na kujifunza kuhusu neema ya Mungu katika kweli. 7 Hii
ndiyo injili mliyojifunza kutoka kwa Epafra, mpendwa wetu mtumishi mwenzetu,
ambaye ni mtumishi mwaminifu wa Kristo kwa niaba yetu. 8 Epafra ameufanya
ujulikane kwetu upendo wenu katika Roho. 9 Kwa sababu ya upendo huu, tangu siku
tuliposikia hivi, hatujaacha kuwaombea. Tumekuwa tukiomba kwamba mtajazwa na
maarifa ya mapenzi yake katika hekima yote na ufahamu wa kiroho. 10 Tumekuwa
tukiomba kwamba mtatembea kwa ustahimilivu wa Bwana katika njia zipendezazo.
Tumekuwa tukiomba kwamba mtazaa tunda katika kila tendo jema na kwamba
mtakua katika maarifa ya Mungu. 11 Tunaomba mweze kutiwa nguvu katika kila
uwezo kulingana na nguvu za utukufu wake katika uvumilivu na ustahimilivu wote.
12 Tunaomba kwamba, kwa furaha, mtatoa shukrani kwa Baba, aliyewafanya ninyi
mweze kuwa na sehemu katika urithi wa waumini katika nuru. 13 Ametuokoa
kutoka katika utawala wa giza na kutuhamishia katika ufalme wa Mwana wake
mpendwa. 14 Katika Mwanae tuna ukombozi, msamaha wa dhambi. 15 Mwana
ni mfano wa Mungu asiyeonekana. Ni mzaliwa wa kwanza wa uumbaji wote.
16 Kwakuwa kwa yeye vitu vyote viliumbwa, vile vilivyoko mbinguni na vilivyoko
duniani, vitu vinavyoonekana na visivyoonekana. ikiwa ni vya enzi au mamlaka au
utawala au wenye nguvu, vitu vyote viliumbwa na yeye na kwa ajili yake. 17 Yeye
amekuwepo kabla ya vitu vyote, na katika yeye vitu vyote vinashikamana pamoja.
18 Na yeye ndiye kichwa cha mwili yaani kanisa, yeye ni mwanzo na mzaliwa wa
kwanza kutoka miongoni mwa wafu, hivyo, ana nafasi ya kwanza miongoni mwa
vitu vyote. 19 Kwa kuwa Mungu alipendezwa kwamba utimilifu wake wote uishi
ndani yake, 20 na kupatanisha vitu vyote kwake kwa njia ya Mwanawe. Mungu
alifanya amani kupitia damu ya msalaba wake. Mungu alipatanisha vitu vyote kwake
mwenyewe, ikiwa ni vitu vya duniani au vitu vya mbinguni. 21 Nanyi pia, kwa
wakati mmoja mlikuwa wageni kwa Mungu na mlikuwa maadui wake katika akili
na matendo maovu. 22 Lakini sasa amewapatanisha ninyi kwa mwili wake kupitia
kifo. Alifanya hivi ili kuwaleta ninyi watakatifu, wasio na lawama na bila dosari
mbele yake, 23 kama mkiendelea katika imani, mliyoimarishwa na kuwa thabiti,
pasipo kuondoshwa mbali kutoka kwenye taraja la ujasiri la injili mliyoisikia. Hi
ndiyo injili iliyotangazwa kwa kila mtu aliyeumbwa chini ya mbingu. Hii ndiyo injili
ambayo kwayo mimi, Paulo, nimekuwa mtumishi. 24 Sasa nafurahia mateso yangu
kwa ajili yenu. Nami natimiliza katika mwili wangu kinachopungua kwa mateso ya
Kristo kwa ajili ya mwili wake, ambao ni kanisa. 25 Mimi ni mtumishi wa kanisa
hili, sawasawa na wajibu niliopewa kutoka kwa Mungu kwa ajili yenu, kulijaza neno
la Mungu. 26 Huu ni ukweli wa siri iliyokuwa imefichwa kwa miaka mingi na kwa
vizazi. Lakini sasa imefunuliwa kwa wote waaminio katika Yeye. 27 Ni kwa wale

ambao Mungu alitaka kufunua kulivyo utajiri wa utukufu wa siri ya ukweli huu
miongoni mwa Mataifa. Ni kwamba Kristo yumo ndani yenu, ujasiri wa utukufu
ujao. [28] Huyu ndiye tunayemtangaza. Tunamwonya kila mtu, na kumfundisha kila
mtu kwa hekima yote, ili kwamba tumlete kila mtu mkamilifu katika Kristo. [29] Kwa
jili hii, mimi najibidisha na kujitahidi kulingana na nguvu yake ifanyayo kazi ndani
yangu katika uweza.

# 2

[1] Kwa kuwa nataka mfahamu jinsi ambavyo nimekuwa na taabu nyingi kwa ajili
yenu, kwa wote walioko Laodikia na kwa wote ambao hawajaona uso wangu katika
mwili. [2] Nafanya kazi ili kwamba mioyo yao iweze kufarijiwa kwa kuletwa pamoja
katika upendo na katika utajiri wote wa wingi wa uhakika kamili wa maarifa, katika
kuijua siri ya kweli ya Mungu, ambaye ni Kristo. [3] Katika Yeye hazina zote za hekima
na maarifa zimefichwa. [4] Nasema hivi ili kwamba mtu yeyote asije akawafanyia
hila kwa hotuba yenye ushawishi. [5] Na ingawa sipo pamoja nanyi katika mwili,
lakini nipo nanyi katika roho. Ninafurahi kuona utaratibu wenu mzuri na nguvu ya
imani yenu katika Kristo. [6] Kama mlivyompokea Kristo Bwana, tembeeni katika yeye.
[7] Mwimarishwe katika yeye, mjengwe katika yeye, mwimarishwe katika imani kama
tu mlivyofundishwa, na kufungwa katika shukrani nyingi. [8] Angalieni ya kwamba
mtu yeyote asiwanase kwa falsafa na maneno matupu ya udanganyifu kulingana na
mapokeo ya wanadamu, kulingana na kanuni za kidunia, na sio kulingana na Kristo.
[9] Kwa kuwa katika yeye ukamilifu wote wa Mungu unaishi katika mwili. [10] Nanyi
mmejazwa katika yeye. Yeye ni kichwa cha kila uweza na mamlaka. [11] Katika yeye
pia mlitahiriwa kwa tohara isiyofanywa na wanadamu katika kuondolewa mwili wa
nyama, lakini ni katika tohara ya Kristo. [12] Mlizikwa pamoja naye katika ubatizo.
Na kwa njia ya imani katika yeye mlifufuliwa kwa uweza wa Mungu, aliyemfufua
kutoka kwa wafu. [13] Na mlipokuwa mmekufa katika makosa yenu na kutokutahiriwa
kwa miili yenu, aliwafanya hai pamoja naye na kutusamehe makosa yetu yote.
[14] Alifuta kumbukumbu ya madeni iliyoandikwa, na taratibu zilizokuwa kinyume
nasi. Aliiondoa yote na kuigongomea msalabani. [15] Aliziondoa nguvu na mamlaka.
Aliyaweka wazi na kuyafanya kuwa sherehe ya ushidi kwa njia ya msalaba wake.
[16] Kwa hiyo, mtu yeyote asiwahukumu ninyi katika kula au katika kunywa, au kuhusu
siku ya sikukuu au mwezi mpya, au siku za Sabato. [17] Hivi ni vivuli vya mambo
yajayo, lakini kiini ni Kristo. [18] Mtu awaye yote asinyang'anywe tuzo yake kwa
kutamani unyenyekevu na kwa kuabudu malaika. Mtu wa jinsi hiyo huingia katika
mambo aliyoyaona na kushawishiwa na mawazo yake ya kimwili. [19] Yeye hakishikilii
kichwa. Ni kutoka katika kichwa kwamba mwili wote kupitia viungo vyake na
mifupa huungwa na kushikamanishwa kwa pamoja; na hukua kwa ukuaji utolewao
na Mungu. [20] Ikiwa mlikufa pamoja na Kristo kwa tabia za dunia, mbona mnaishi
kama mnawajibika kwa dunia: [21] “Msishike, wala kuonja, wala kugusa”? [22] Haya
yote yameamuriwa kwa ajili ya uharibifu ujao na matumizi, kutokana na maelekezo
na mafundisho ya wanadamu. [23] Sheria hizi zina hekima ya dini zilizotengenezwa
kwa ubinafsi na unyenyekevu na mateso ya mwili. Lakini hazina thamani dhidi ya
tamaa za mwili.

# 3

[1] Ikiwa tena Mungu amewafufua pamoja na Kristo, yatafuteni mambo ya juu
ambako Kristo anakaa mkono wa kuume wa Mungu. [2] Fikirini kuhusu mambo ya juu,
sio kuhusu mambo ya duniani. [3] Kwa kuwa mmekufa, na maisha yenu yamefichwa
pamoja na Kristo katika Mungu. [4] Wakati Kristo atakapoonekana, ambaye ni maisha

yenu, ndipo nanyi pia mtaonekana naye katika utukufu. 5 Kwa hiyo yafisheni
mambo yaliyo katika nchi yaani, zinaa, uchafu, shauku mbaya, nia mbaya, na tamaa,
ambayo ni ibada ya sanamu. 6 Ni kwa ajili ya mambo haya ghadhabu ya Mungu
inakuja juu ya wana wasio tii. 7 Ni kwa ajili ya mambo haya ninyi pia mlitembea
kwayo mlipoishi kati yao. 8 Lakini sasa ni lazima myaondoe mambo haya yote.
Yaani, ghadhabu, hasira, nia mbaya, matusi, na maneno machafu yatokayo vinywani
mwenu. 9 Msidanganyane ninyi kwa ninyi, kwa kuwa mmeuvua utu wenu wa kale
na matendo yake. 10 Mmevaa utu mpya, ambao unafanywa upya katika maarifa
kutokana mfano wa yule aliye muumba. 11 Katika maarifa haya, hakuna Myunani
na Myahudi, kutahiriwa na kutokutahiriwa, msomi, asiye msomi, mtumwa, asiye
mtumwa, lakini badala yake Kristo ni mambo yote katika yote. 12 Kama wateule
wa Mungu, watakatifu na wapendwao, jivikeni utu wema, ukarimu, unyenyekevu,
upole na uvumilivu. 13 Chukulianeni ninyi kwa ninyi. Hurumianeni kila mtu na
mwenzake. Kama mtu analalamiko dhidi ya mwingine, amsamehe kwa jinsi ilele
ambayo Bwana alivyo wasamehe ninyi. 14 Zaidi ya mambo haya yote, muwe na
upendo, ambao ndio kigezo cha ukamilifu. 15 Amani ya Kristo na iwaongoze mioyoni
mwenu. Ilikuwa ni kwa ajili ya amani hii kwamba mliitiwa katika mwili mmoja.
Iweni na shukrani. 16 Na Neno la Kristo likae ndani yenu kwa utajiri. Kwa hekima
yote, fundishaneni na kushauriana ninyi kwa ninyi kwa Zaburi, nyimbo, na nyimbo
za rohoni. Imbeni kwa shukrani mioyo yenu kwa Mungu. 17 Na chochote mfanyacho,
katika maneno au katika matendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu. Mpeni
shukrani Mungu baba kupitia Yeye. 18 Wake, wanyenyekeeni waume zenu, kama
ipendezavyo katika Bwana. 19 Nanyi waume, wapendeni wake zenu, na msiwe
wakali dhidi yao. 20 Watoto, watiini wazazi wenu katika mambo yote, maana ndivyo
impendezavyo Bwana. 21 Akina baba msiwachokoze watoto wenu, ili kwamba wasije
wakakata tamaa. 22 Watumwa, watiini mabwana zenu katika mwili kwa mambo yote,
sio kwa huduma ya macho kama watu wa kufurahisha tu, bali kwa moyo wa kweli.
Mwogopeni Mungu. 23 Chochote mfanyacho, fanyeni kutoka nafsini mwenu kama
kwa Bwana na si kama kwa wanadamu. 24 Mnajua ya kwamba mtapokea tuzo ya
umilkaji kutoka kwa Bwana. Ni Kristo Bwana mnayemtumikia. 25 Kwa sababu yeyote
atendaye yasiyo haki atapokea hukumu kwa matendo yasiyo haki aliyoyafanya, na
hakuna upendeleo.

# 4

1 Mabwana, toeni kwa watumwa mambo yaliyo haki na ya adili. Mnajua pia
kwamba mnaye Bwana mbinguni. 2 Endeleeni kuwa thabiti katika maombi. Kaeni
macho katika hilo kwa shukrani. 3 Ombeni pamoja kwa ajili yetu pia, ili kwamba
Mungu afungue mlango kwa ajili ya neno, kunena siri ya ukweli ya Kristo. Kwa
sababu ya hili nimefungwa minyororo. 4 Na ombeni kwamba niweze kuliweka
wazi, kama inavyonipasa kusema. 5 Enenda kwa hekima kwa wale walioko nje, na
muukomboe wakati. 6 Maneno yenu na yawe na neema wakati wote, na yakolee
chumvi majira yote, ili kwamba mweze kujua jinsi inavyowapasa kumjibu kila
mtu. 7 Kwa mambo yanayonihusu mimi, Tikiko atayafanya yajulikane kwenu. Yeye
ni ndugu mpendwa, mtumishi mwaminifu, na mtumwa mwenzetu katika Bwana.
8 Namtuma kwenu kwa ajili ya hili, kwamba mweze kujua mambo kuhusu sisi na
pia kwamba aweze kuwatia moyo. 9 Namtuma pamoja na Onesimo, ndugu yetu
mpendwa mwaminifu, na mmoja wenu. Watawaambia kila kitu kilichotokea hapa.
10 Aristarko, mfungwa mwenzangu, anawasalimu, pia na Marko binamu yake na
Barnaba mliyepokea utaratibu kutoka kwake, “kama akija kwenu, mpokeeni,” 11 Na
pia Yesu aitwaye Yusto. Hawa peke yao wa tohara ni watendakazi wenzangu kwa

jili ya ufalme wa Mungu. Wamekuwa ni faraja kwangu. 12 Epafra anawasalimu.
Yeye ni mmoja wenu na mtumwa wa Kristo Yesu. Yeye hufanya bidii katika maombi
kwa ajili, ili kwamba mweze kusimama kwa ukamilifu na kuhakishwa kikamilifu
katika mapenzi yote ya Mungu. 13 Kwa kuwa ninamshuhudia, kwamba anafanya
kazi kwa bidii kwa ajili yenu, kwa hao walioko Laodekia, na kwa hao walioko
Hierapoli. 14 Luka yule tabibu mpendwa, na Dema wanawasalimu. 15 Wasalimu
ndugu zangu walioko Laodekia, na Nimfa, na kanisa lile lililoko nyumbani kwake.
16 Barua hii itakapokuwa imesomwa miongoni mwenu, isomwe pia kwa kanisa la
walaodekia, nanyi pia hakikisheni mnaisoma ile barua kutoka Laodekia. 17 Sema kwa
Arkipo, ''Angalia ile huduma ambayo umeipokea katika Bwana, kwamba unapaswa
kuitimiza.” 18 Salamu hii ni kwa mkono wangu mwenyewe - Paulo. Ikuumbukeni
minyororo yangu. Neema na iwe nanyi.

# 1 Wathesalonike

1 Paulo, Silwano na Timotheo kwa kanisa la Wathesalonike katika Mungu Baba
na Bwana Yesu Kristo. Neema na amani iwe nanyi. 2 Tunatoa shukrani kwa
Mungu kila mara kwa ajili yenu nyote, wakati tunapowataja katika maombi yetu.
3 Tunaikumbuka bila kukoma mbele ya Mungu na baba yetu kazi yenu ya imani,
juhudi ya upendo, na uvumilivu wenye ujasiri kwa ajili ya baadaye katika Bwana
Yesu Kristo. 4 Ndugu Mnaopendwa na Mungu, tunajua wito wenu. 5 Na jinsi injili
yetu ilivyokuja kwenu si kwa neno tu, bali pia katika nguvu, katika Roho Mtakatifu,
na katika uhakika. Kwa namna hiyo, mnajua pia sisi tulikuwa watu wa namna
gani miongoni mwenu kwa ajili yenu. 6 Mlikuwa watu wa kutuiga sisi na Bwana,
kama mlivyopokea neno katika taabu kwa furaha itokayo kwa Roho Mtakatifu.
7 Na matokeo yake, mkawa mfano kwa wote katika Makedonia na Akaiya ambao
wanaamini. 8 Kwa kuwa kutoka kwenu neno la Mungu limeenea kote, na si kwa
Mekadonia na Akaiya peke yake. Badala yake, kwa kila mahali imani yenu katika
Mungu imeenea kote. Na matokeo yake, hatuhitaji kusema chochote. 9 Kwa kuwa
wao wenyewe wanaarifu ujio wetu ulikuwa wa namna gani kati yenu. Wanasimulia
jinsi mulivyomgeukia Mungu kutoka katika sanamu na kumtumikia Mungu aliye hai
na wa kweli. 10 Walitoa habari kuwa mnamsubiri Mwana wake kutoka mbinguni,
aliyefufuliwa kutoka kwa wafu. Na huyu ni Yesu, anayetuweka huru kutoka kwenye
ghadhabu ijayo.

## 2

1 Kwa kuwa ninyi wenyewe mnajua, ndugu, kuwa ujio wetu kwenu haukuwa
wa bure. 2 Mnajua kwamba mwanzoni tuliteseka na walitutenda kwa aibu kule
Filipi, kama mujuavyo. Tulikuwa na ujasiri katika Mungu kunena injili ya Mungu
hata katika taabu nyingi. 3 Kwa maana mahusia yetu hayatokani na ubaya, wala
katika uchafu, wala katika hila. 4 Badala yake, kama vile tulivyokubalika na Mungu
na kuaminiwa injili, ndivyo tunenavyo. Tunanena, si kwa kuwafurahisha watu,
lakini kumfurahisha Mungu. Yeye pekee ndiye achunguzaye mioyo yetu. 5 Kwa
maana hatukutumia maneno ya kujipendekeza wakati wote wote, kama mjuavyo,
wala ukutumia maneno kama kisingizio kwa tamaa, Mungu ni shahidi wetu. 6 Wala
hatukutafuta utukufu kwa watu, wala kutoka kwenu au kwa wengine. Tungeweza
kudai kupendelewa kama mitume wa Kristo. 7 Badala yake tulikuwa wapole kati
yenu kama mama awafarijivyo watoto wake mwenyewe. 8 Kwa njia hii tulikuwa
na upendo kwenu. Tulikuwa radhi kuwashirikisha si tu injili ya Mungu bali pia na
maisha yetu wenyewe. Kwa kuwa mmekuwa wapendwa wetu. 9 Kwa kuwa ndugu,
mnakumbuka kazi na taabu yetu. Usiku na mchana tulikuwa tukifanya kazi kusudi
tusije tukamlemea yeyote. Wakati huo, tuliwahubiria injili ya Mungu. 10 Ninyi ni
mashahidi, na Mungu pia, ni kwa utakatifu wa namna gani, haki, na bila lawama
tulivyoenenda wenyewe mbele yenu mnaoamini. 11 Vivyo hivyo, mnajua ni kwa
namna gani kwa kila mmoja wenu, kama baba alivyo kwa wanawe tulivyowahimiza
na kuwatia moyo. Tulishuhudia 12 kwamba mlipaswa kuenenda kama ulivyo mwito
wenu kwa Mungu, aliyewaita kwenye ufalme na utukufu wake. 13 Kwa sababu hiyo
twamshukuru Mungu pia kila wakati. Kwa kuwa wakati mlipo pokea kutoka kwetu
ujumbe wa Mungu mliosikia, mlipokea si kama neno la wanadamu. Badala yake,
mlipokea kama kweli ilivyo, neno la Mungu. Ni neno hili ambalo linalofanya kazi
kati yenu mnaoamini. 14 Kwa hivyo ninyi, ndugu, muwe watu wa kuiga makanisa ya

Mungu yaliyoko katika Uyahudi katika Kristo Yesu. Kwa kuwa ninyi pia mliteseka
katika mambo yale yale kutoka kwa watu wenu, kama ilivyo kuwa kutoka kwa
wayahudi. 15 walikuwa ni Wayahudi ndiyo waliomuua Bwana Yesu pamoja na
manabii. Ni Wayahudi ambao walitufukuza tutoke nje. Hawampendezi Mungu na
ni maadui kwa watu wote. 16 Walituzuia tusiseme na Mataifa ili wapate kuokolewa.
Matokeo yake ni kwamba wanaendelea na dhambi zao. Mwisho ghadhabu imekuja
juu yao. 17 Sisi, ndugu, tulikuwa tumetengana nanyi kwa muda mfupi, kimwili, si
katika roho. Tulifanya kwa uwezo wetu na kwa shauku kuu kuona nyuso zenu.
18 Kwa kuwa tulitaka kuja kwenu, mimi Paulo, kwa mara moja na mara nyingine,
lakini shetani alituzuia. 19 Kwa kuwa kujiamini kwetu ni nini kwa baadaye, au furaha,
au taji ya kujivunia mbele za Bwana wetu Yesu wakati wa kuja kwake? Je si ninyi
zaidi kama walivyo wengine? 20 Kwa kuwa ninyi ni utukufu na furaha yetu.

# 3

1 Kwa hiyo, tulipo kuwa hatuwezi kuvumilia zaidi, tulifikiri kuwa ilikuwa vema
kubaki kule Athene peke yetu. 2 Tulimtuma Timotheo, ndugu yetu na mtumishi wa
Mungu katika injili ya Kristo, kuwaimalisha na kuwafariji kuhusiana na imani yenu.
3 Tulifanya haya ili kusudi asiwepo yeyote wa kuteteleka kutokana na mateso haya,
kwa kuwa wenyewe mnajua kwamba tumekwisha teuliwa kwa ajili ya hili. 4 Kwa
kweli, wakati tulipokuwa pamoja nanyi, tulitangulia kuwaeleza ya kuwa tulikuwa
karibu kupata mateso, na hayo yalitokea kama mjuavyo. 5 Kwa sababu hii, nilipo
kuwa siwezi kuvumilia tena, nilituma ilikusudi nipate kujua juu ya imani yenu.
Huenda mjaribu alikuwa angalau amewajaribu, na kazi yetu ikawa ni bure. 6 Lakini
Timotheo alikuja kwetu kutokea kwenu na akatuletea habari njema juu ya imani na
upendo wenu. Alitwambia ya kuwa mnayo kumbukumbu nzuri juu yetu, na kuwa
mnatamani kutuona kama ambavyo nasi twatamani kuwaona ninyi. 7 Kwa sababu
hii, ndugu tulifarijika sana na ninyi kwa sababu ya imani yenu, katika taabu na
mateso yetu yote. 8 Kwa sasa tunaishi, kama mkisimama imara kwa Bwana, 9 Kwani
ni shukurani zipi tumpe Mungu kwa ajili yenu, kwa furaha yote tuliyonayo mbele
za Mungu juu yenu? 10 Tunaomba sana usiku na mchana ili tuweze kuziona nyuso
zenu na kuwaongezea kinachopungua katika imani yenu. 11 Mungu wetu na Baba
mwenyewe, na Bwana wetu Yesu atuongoze njia yetu tufike kwenu. 12 Na Bwana
awafanye muongezeke na kuzidi katika pendo, mkipendana na kuwapenda watu
wote, kama tunavyowafanyia ninyi. 13 Na afanye hivi ili kuiimarisha mioyo yenu
iwe bila lawama katika utakatifu mbele za Mungu wetu na Baba yetu katika ujio wa
Bwana Yesu pamoja na watakatifu wake wote.

# 4

1 Hatimaye, ndugu, twawatia moyo na kuwasihi kwa Yesu Kristo. Kama
mlivyopokea maelekezo toka kwetu namna iwapasavyo kuenenda na kumpendeza
Mungu, kwa njia hiyo pia muenende na kutenda zaidi. 2 Kwa kuwa mwajua ni
maelekezo gani tuliyowapa kupitia Bwana Yesu. 3 Kwa kuwa haya ndiyo mapenzi ya
Mungu: utakaso wenu - kwamba muepuke zinaa, 4 Kwamba kila mmoja wenu anajua
namna ya kumiliki mke wake mwenyewe katika utakatifu na heshima. 5 Usiwe na
mke kwa ajili ya tamaa za mwili (kama Mataifa wasiomjua Mungu). 6 Asiwepo
mtu yeyote atakaye vuka mipaka na kumkosea nduguye kwa ajili ya jambo hili.
Kwa kuwa Bwana ndiye mwenye kulipa kisasi kwa mambo yote haya, kama tulivyo
tangulia kuwaonya na kushuhudia. 7 Kwa kuwa Bwana hakutuita kwa uchafu,
bali kwa utakatifu. 8 Kwa hiyo anayelikataa hili hawakatai watu, bali anamkataa
Mungu, anayewapa Roho Mtakatifu wake. 9 Kuhusu upendo wa ndugu, hakuna

haja ya mtu yeyote kukuandikia, kwa kuwa mmefundishwa na Mungu kupendana
ninyi kwa ninyi. 10 Hakika, mlifanya haya yote kwa ndugu walioko Makedonia
yote, lakini twawasihi, ndugu, mfanye hata na zaidi. 11 Twawasihi mtamani kuishi
maisha ya utulivu, kujali shughuli zenu, na kufanya kazi kwa mikono yenu, kama
tulivyowaamuru. 12 Fanya haya ili uweze kuenenda vizuri na kwa heshima kwa
hao walio nje ya imani, ili usipungukiwe na hitaji lolote. 13 Hatutaki ninyi muelewe
isivyo sahihi, enyi ndugu, juu ya hao waliolala, ili msije mkahuzunika kama wengine
wasio na uhakika kuhusu wakati ujao. 14 Iwapo tunaamini kuwa Yesu alikufa na
akafufuka tena, vivyo hivyo Mungu atawaleta pamoja na Yesu hao waliolala mauti
katika yeye. 15 Kwa ajili ya hayo twawaambia ninyi kwa neno la Bwana, kwamba sisi
tulio hai, tutakaokuwepo wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia
wale waliolala mauti. 16 Kwa kuwa Bwana mwenyewe atashuka toka mawinguni.
Atakuja na sauti kuu, pamoja na sauti ya malaika mkuu, pamoja na parapanda
ya Mungu, nao waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza. 17 Kisha sisi tulio hai,
tuliobaki, tutaungana katika mawingu pamoja nao kumlaki Bwana hewani. Kwa
njia hii tutakuwa na Bwana siku zote. 18 Kwa hiyo, mfarijiane ninyi kwa ninyi kwa
maneno haya.

# 5

1 Sasa, kwa habari ya muda na nyakati, ndugu, hamna haja kwamba kitu chochote
kiandikwe kwenu. 2 Kwa kuwa ninyi wenyewe mwajua kwa usahihi ya kuwa siku ya
Bwana inakuja kama mwizi ajapo usiku. 3 Pale wasemapo kuna “Amani na usalama”,
ndipo uharibifu huwajia ghafla. Ni kama utungu umjiavyo mama mwenye mimba.
Hawataepuka kwa njia yeyote. 4 Lakini ninyi, ndugu hampo kwenye giza hata ile
siku iwajie kama mwizi. 5 Kwa maana ninyi nyote ni wana wa nuru na wana wa
mchana. Sisi siyo wana wa usiku au wa gizani. 6 Hivyo basi, tusilale kama wengine
walalavyo. Bali tukeshe na kuwa makini. 7 Kwa kuwa wanaolala hulala usiku na
wanao lewa hulewa usiku. 8 Kwa kuwa sisi ni wana wa mchana, tuwe makini.
Tuvae ngao ya imani na upendo, na, kofia ya chuma, ambayo ni uhakika wa wokovu
wa wakati ujao. 9 Kwa kuwa Mungu hakutuchagua mwanzo kwa ajili ya gadhabu,
bali kwa kupata wokovu kwa njia ya Bwana Yesu Kristo. 10 Yeye ndiye aliyetufia ili
kwamba, tukiwa macho au tumelala, tutaishi pamoja naye. 11 Kwa hiyo, farijianeni na
kujengana ninyi kwa ninyi, kama ambavyo tayari mnafanya. 12 Ndugu, twawaomba
muwatambue wale wanaotumika miongoni mwenu na wale walio juu yenu katika
Bwana na wale wanao washauri. 13 Tunawaomba pia muwatambue na kuwapa
heshima katika upendo kwa sababu ya kazi yao. Muwe na amani miongoni mwenu
ninyi wenyewe. 14 Twawasihi, ndugu: muwaonye wasio kwenda kwa utaratibu,
watieni moyo walio kata tamaa, Wasaidieni walio wanyonge, na muwe wavumilivu
kwa wote. 15 Angalieni asiwepo mtu yeyote anayelipa baya kwa baya kwa mtu
yeyote. Badala yake, fanyeni yaliyo mema kwa kila mmoja wenu na kwa watu
wote. 16 Furahini siku zote. 17 Ombeni bila kukoma. 18 Mshukuruni Mungu kwa
kila jambo, kwa sababu hayo ndiyo mapenzi ya Mungu kwenu katika Yesu Kristo.
19 Msimzimishe Roho. 20 Msiudharau unabii. 21 Yajaribuni mambo yote. Mlishike lililo
jema. 22 Epukeni kila mwonekano wa uovu. 23 Mungu wa amani awakamilishe katika
utakatifu. Roho, nafsi na mwili vitunzwe pasipo mawaa katika kuja kwake Bwana
wetu Yesu Kristo. 24 Yeye aliyewaita ni mwaminifu, naye ndiye mwenye kutenda.
25 Ndugu, tuombeeni pia. 26 Wasalimuni ndugu wote kwa busu takatifu. 27 Nawasihi
katika Bwana kwamba barua hii isomwe kwa ndugu wote. 28 Neema ya Bwana wetu
Yesu Kristo iwe pamoja nanyi.

# 2 Wathesalonike

1 Paulo, Silwano, na Timotheo, kwa kanisa la Wathesalonike katika Mungu Baba
yetu na Bwana Yesu Kristo. 2 Neema na iwe kwenu na amani itokayo kwa Mungu
Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo. 3 Imetupasa sisi kumshukuru Mungu siku
zote kwa ajili yenu, ndugu. Maana hivi ndivyo itupasavyo, kwa kuwa imani yenu
inakua sana, na upendo wenu kwa kila mtu uongezeke mwingi. 4 Hivyo sisi wenyewe
tunaongea kwa fahari juu yenu katika makanisa ya Mungu. Tunazungumza habari
ya saburi yenu na imani mliyo nayo katika mateso yote. Tunaongea kwa habari ya
mateso mnayostahimili. 5 Hii ndiyo ishara ya hukumu ya haki ya Mungu. Matokeo
ya haya ni kuwa ninyi mhesabiwe kuwa mwastahili kuuingia ufalme wa Mungu
ambao kwa ajili yake mnateswa. 6 Kwa kuwa ni haki kwa Mungu kuwalipa mateso
wale wawatesao ninyi, 7 na kuwapa raha ninyi mteswao pamoja nasi. Atafanya hivi
wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa
uweza wake. 8 Katika mwali wa moto atawalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu
na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu. 9 Watateseka kwa maangamizi ya
milele wakiwa wametengwa na uwepo wa Bwana na utukufu wa nguvu zake.
10 Atafanya wakati atakapokuja ili kutukuzwa na watu wake na kustaajabishwa na
wote walioamini. Kwa sababu ushuhuda wetu kwenu ulisadikiwa kwenu. 11 Kwa
sababu hii twawaombea ninyi siku zote. Twaomba kwamba Mungu wetu awahesabu
kuwa mlistahili kuitwa. Twaomba kwamba apate kutimiza kila haja ya wema na kila
kazi ya imani kwa nguvu. 12 Tunaomba mambo haya ili mpate kulitukuza jina la
Bwana Yesu. Tunaomba kwamba mpate kutukuzwa naye, kwa sababu ya neema ya
Mungu na ya Bwana Yesu Kristo.

## 2

1 Sasa kuhusu kuja kwa Bwana wetu Yesu Kristo na kukusanywa pamoja ili tuwe
naye: tunawaomba ninyi ndugu zetu, 2 kwamba msisumbuliwe wala kutabishwa
kwa urahisi, kwa roho, au kwa ujumbe au kwa barua inayoonkana kuwa imetoka
kwetu, ikisema ya kuwa siku ya Bwana tayari imekuja. 3 Mtu na asiwadanganye
kwa namna yoyote. Kwa kuwa haitakuja mpaka lile anguko litokee kwanza
na mtu wa uasi afunuliwe, yule mwana wa uharibifu. 4 Huyu ndiye apingaye
naye hujiinua mwenyewe akimpinga Mungu na chochote kinachoabudiwa. Na
matokeo yake, hukaa kwenye hekalu la Mungu na kujionyesha yeye kuwa kama
Mungu. 5 Je, hamkumbuki kuwa nilipokuwa nanyi niliwaambia juu ya mambo haya?
6 Sasa mnajua kile kinachomzuia, ili kwamba aweze kufunuliwa kwa wakati sahihi
utakapowadia. 7 Kwa kuwa siri ya yule mtu mwenye kuasi inafanya kazi mpaka sasa,
ila tu kuna anaye mzuia sasa mpaka atakapotolewa njiani. 8 Ndipo yule mwenye
kuasi atakapofunuliwa, amabaye Bwana Yesu atamwua kwa pumzi ya kinywa chake.
Bwana atamfanya kuwa si chochote kwa ufunuo wa ujio wake. 9 Ujio wa yule mwenye
kuasi utakuwa kwa sababu ya kazi ya shetani kwa nguvu zote, ishara na maajabu
ya uongo, 10 na uongo wote wenye udhalimu. Mambo haya yatakuwepo kwa wale
wanaopotea, kwa sababu hawakuupokea upendo wa kweli kwa ajili ya kuokolewa
kwao. 11 Kwa sababu hiyo Mungu anawatumia kazi yenye uovu ili waamini uongo.
12 Matokeo yake ni kwamba wote watahukumiwa, wale ambao hawakuamini ukweli
bali wao hujifurahisha katika udhalimu. 13 Lakini inatupasa tumshukuru Mungu kila
mara kwa ajili yenu ndugu mpendwao na Bwana. Kwa sababu Bwana aliwachagua
ninyi kama malimbuko ya wokovu kwa utakaso wa Roho na imani katika ile kweli.

[14] Hiki ndicho alichowaitieni ninyi, kwamba kupitia injili muweza kuupata utukufu
wa Bwana wetu Yesu Kristo. [15] Kwa hiyo, ndugu, simameni imara. Ueleweni ule
utamaduni mliofundishwa, kwa neno au kwa barua yetu. [16] Sasa, Bwana wetu Yesu
Kristo mwenyewe, na Mungu Baba yetu aliyetupenda na kutupa faraja ya milele na
ujasiri mwema kwa ajili ya maisha yajayo kupitia neema, [17] awafariji na kuifanya
imara mioyo yenu katika kila neno na kazi njema.

# 3

[1] Na sasa, ndugu, tuombeeni, kwamba neno la Bwana liweze kuenea na kutukuzwa,
kama ilivyo pia kwenu. [2] Ombeni kwamba tuweze kuokolewa kutoka katika uovu
na watu waasi, kwa kuwa si wote wana imani. [3] Lakini Bwana ni mwaminifu,
ambaye atawaimarisha ninyi na kuwalinda kutoka kwa yule mwovu. [4] Tunaujasiri
katika Bwana kwa ajili yenu, kwamba mnatenda na mtaendelea kutenda mambo
ambayo tunawaagiza. [5] Bwana aweze kuongoza mioyo yenu katika upendo na katika
uvumilivu wa Kristo. [6] Sasa tunawaagiza, ndugu, katika jina la Bwana Yesu Kristo,
kwamba mwepuke kila ndugu ambaye anaishi maisha ya uvivu na siyo kwa kutokana
na desturi ambazo mlipokea kutoka kwetu. [7] Kwa kuwa ninyi wenyewe mnajua ni
sawa kwenu kutuiga sisi. Hatukuishi miongoni mwenu kama wale ambao hawakuwa
na nidhamu. [8] Na hatukula chakula cha mtu yeyote bila kukilipia. Badala yake,
tulifanya kazi usiku na mchana kwa kazi ngumu na kwa shida, ili tusiweze kuwa
mzigo kwa yeyote katika ninyi. [9] Tulifanya hivi si kwa sababu hatuna mamlaka.
Badala yake, tulifanya hivi ili tuwe mfano kwenu, ili kwamba mweze kutuiga sisi.
[10] Wakati tulipokuwa pamoja nanyi tuliwaagiza, “Ikiwa mmoja wenu hataki kufanya
kazi, na asile.” [11] Kwa kuwa tunasikia kwamba baadhi wanaenenda kwa uvivu
miongoni mwenu. Hawafanyi kazi lakini badala yake ni watu wasio na utaratibu.
[12] Sasa hao nao tunaagiza na kuwaasa katika Bwana Yesu Kristo, kwamba lazima
wafanye kazi kwa utulivu na kula chakula chao wenyewe. [13] Lakini ninyi, ndugu,
msizimie roho katika kufanya yaliyo sahihi. [14] Ikiwa mtu yeyote hataki kutii neno letu
katika waraka huu, mwe makini naye na msiwe na ushirika pamoja naye, ili kwamba
aweze kuaibika. [15] Msimchukulie kama adui, lakini mwonyeni kama ndugu. [16] Bwana
wa amani mwenyewe awape amani wakati wowote katika njia zote. Bwana awe
nanyi nyote. [17] Hii ni salam yangu, Paulo, kwa mkono wangu mwenyewe, ambayo ni
alama katika kila waraka. Hivi ndivyo niandikavyo. [18] Neema ya Bwana wetu Yesu
Kristo iweze kuwa nanyi nyote.

# 1Timotheo

1 Paulo, Mtume wa Kristo Yesu, kulingana na amri ya Mungu na Mwokozi wetu
Yesu Kristo aliye ujasiri wetu, 2 kwa Timotheo mwanangu wa kweli katika imani:
Neema, rehema na amani zitokazo kwa Mungu Baba na Kristo Yesu Bwana wetu.
3 Kama nilivyokusihi nilipoondoka kwenda Makedonia, ubaki Efeso ili kwamba
uweze kuwaamru watu fulani wasifundishe mafundisho tofauti. 4 Pia wasisikilize
hadithi na orodha za nasaba zisizo na mwisho. Haya husababisha mabishano
zaidi kuliko kuwasaidia kuendeleza mpango wa Mungu wa imani. 5 Basi lengo la
agizo hili ni upendo utokao katika moyo safi, katika dhamiri nzuri na katika imani
ya kweli. 6 Baadhi ya watu wamelikosa lengo wakayaacha mafundisho haya na
kugeukia mazungumzo ya kipumbavu. 7 Wanataka kuwa waalimu wa sheria, lakini
hawafahamu wanachosema au wanachosisitiza. 8 lakini tunajua kwamba sheria ni
njema kama mtu ataitumia kwa usahihi. 9 Tunajua kuwa, sheria haikutungwa kwa
ajili ya mtu mwenye haki, bali kwa ajili ya wavunja sheria na waasi, watu wasio
wataua na wenye dhambi, na ambao hawana Mungu na waovu. Imetungwa kwa
ajili ya wauao baba na mama zao, kwa ajili ya wauaji, 10 kwa ajili ya waasherati, kwa
ajili ya watu wazinzi, kwa ajili ya wale wanaoteka watu na kuwafanya watumwa,
kwa ajili ya waongo, kwa ajili ya mashahidi wa uongo, na yeyote aliye kinyume na
maelekezo ya uaminifu. 11 Malekezo haya yanatokana na injili yenye utukufu ya
Mungu mwenye kubarakiwa ambayo kwayo nimeaminiwa. 12 Ninamshukuru Yesu
Kristo Bwana wetu. Alinitia nguvu, kwa kuwa alinihesabu mimi kuwa mwaminifu,
na akaniweka katika huduma. 13 Nilikuwa mtu wa kukufuru, mtesaji na mtu wa
vurugu. Lakini nilipata rehema kwa sababu nilitenda kwa ujinga kwa kutoamini.
14 Lakini neema ya Mungu wetu imejaa imani na upendo ulio katika Kristo Yesu.
15 Ujumbe huu ni wa kuaminika na unastahili kupokelewa na wote, ya kuwa Kristo
Yesu alikuja duniani kuokoa wenye dhambi. Mimi ni mbaya zaidi ya wote. 16 Lakini
kwa sababu hii mimi nilipewa rehema ili kwamba ndani yangu mimi, awali ya
yote, Kristo Yesu adhihirishe uvumilivu wote. Alifanya hivyo kama kielelezo kwa
wote watakaomtumaini Yeye kwa ajili ya uzima wa milele. 17 Na sasa kwa Mfalme
asiye na ukomo, asiyekufa, asiyeonekana, Mungu pekee, iwe heshima na utukufu
milele na milele. Amina. 18 Ninaliweka agizo hili mbele yako Timotheo, mtoto
wangu. Nafanya hivi kulingana na unabii uliotolewa hapo kwanza kukuhusu wewe,
ili kwamba uhusike katika vita njema. 19 Fanya hivyo ili kwamba uwe na imani na
dhamiri njema. Baadhi ya watu wameyakataa haya wakaangamiza imani. 20 Kama
vile Himeneyo na Alekizanda ambao nimempa shetani ili wafundishwe wasikufuru.

## 2

1 Kwa hiyo awali ya yote, nahitaji maombi, na dua, na maombezi, na shukrani
vifanyike kwa ajili ya watu wote, 2 kwa ajili ya wafalme na wote ambao wako kwenye
mamlaka, ili kwamba tuweze kuishi maisha ya amani na utulivu katika utauwa wote
na heshima. 3 Hili ni jema na lenye kukubalika mbele za Mungu Mwokozi wetu.
4 Yeye hutamani kuwa watu wote waokolewe na wapate kuijua kweli. 5 Kwa kuwa
kuna Mungu mmoja, na kuna mpatanishi mmoja kati ya Mungu na mwanadamu
ambaye ni Kristo Yesu. 6 Alijitoa mwenyewe kama fidia kwa wote, kama ushuhuda
kwa wakati muafaka. 7 Kwa sababu hii, mimi mwenyewe nilifanywa kuwa mjumbe
wa injili na mtume. Nasema kweli. Sisemi uongo. Mimi ni mwalimu watu Mataifa
katika imani na kweli. 8 Kwa hiyo, nataka wanaume kila mahali waombe na kuinua

mikono mitakatifu bila ghadhabu na mashaka. 9 Vivyo hivyo, nataka wanawake
wajivike mavazi yanayokubalika, kwa heshima na kujizuia. Wasiwe na nywele
zilizosukwa, au dhahabu, au Lulu, au mavazi ya gharama kubwa. 10 Pia nataka wavae
mavazi yanayowastahili wanawake wanaokiri uchaji kwa kupitia matendo mema.
11 Mwanamke na ajifunze katika hali ya utulivu na kwa utii wote. 12 Simruhusu
mwanamke kufundisha, au kuwa na mamlaka juu ya mwanaume bali aishi katika
hali ya ukimya. 13 Kwa kuwa Adamu aliumbwa kwanza, kisha Eva. 14 Adamu
hakudanganywa, lakini mwanamke alidanganywa kabisa katika uasi. 15 Hata hivyo,
ataokolewa kwa kupitia kuzaa watoto, kama wataendelea katika imani na upendo na
katika utakaso na akili njema.

# 3

1 Usemi huu ni wakuaminika: Kama mtu anatamani kuwa Msimamizi, anatamani
kazi njema. 2 Kwa hiyo msimamizi ni lazima asiwe na lawama. Ni lazima
awe mume wa mke mmoja. Ni lazima awe na kiasi,, busara, mwenye utaratibu,
mkarimu. Ni lazima awe uwezo wa kufundisha. 3 Asiwe anatumia mvinyo, asiwe
mgomvi, bali mpole, mwenye amani. Ni lazima asiwe mwenye kupenda fedha.
4 Inampasa kuwasimamia vema watu wa nyumbani mwake mwenyewe, na watoto
wake imewapasa kumtii kwa heshima zote. 5 Maana ikiwa mtu hajui kuwasimamia
watu wa nyumbani mwake mwenyewe, atalileaje kanisa la Mungu? 6 Asiwe mwamini
mpya, ili kwamba asije akajivuna na kuanguka katika hukumu kama yule mwovu.
7 Lazima pia awe na sifa njema kwa wote walioko nje, ili asije akaanguka kwenye
aibu na mtego wa mwovu. 8 Mashemasi, vilevile wanapaswa kuwa wenye kustahili
heshima, wasiwe wenye kauli mbili. Wasitumie mvinyo kupita kiasi au kuwa na
tamaa. 9 Waweze kuitunza kwa dhamiri safi ile kweli ya imani iliyofunuliwa. 10 Wawe
pia wamethibitishwa kwanza, halafu waweze kuhudumu kwa sababu hawana
lawama. 11 Wanawake vivyo hivyo wawe wenye heshima. Wasiwe wasingiziaji.
Wawe na kiasi na waaminifu kwa mambo yote. 12 Mashemasi ni lazima wawe
waume wa mke mmoja mmoja. Lazima waweze kuwasimamia vema watoto wao
na wa nyumbani mwao. 13 Kwa kuwa wale wanaotumika vizuri hupata msimamo
mzuri na ujasiri mkubwa katika imani iliyo katika Kristo Yesu. 14 Ninaandika mambo
haya kwako, na ninatumaini kuja kwako hivi karibuni. 15 Lakini ikiwa nitachelewa,
ninaandika ili upate kujua namna ya kuenenda katika nyumba ya Mungu, ambalo
ni kanisa la Mungu aliye hai, nguzo na msaada wa kweli. 16 Na haipingiki kwamba
kweli ya Uungu uliyofunuliwa ni mkuu: "Alionekana katika mwili, akathibitishwa
na Roho, akaonekana na malaika, akatangazwa miongoni mwa mataifa, akaaminiwa
na ulimwengu, na akachukuliwa juu katika utukufu."

# 4

1 Sasa Roho anasema waziwazi kwamba katika nyakati zijazo baadhi ya watu
wataiacha imani na kuwa makini kusikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya
kipepo yatakayofundishwa 2 katika uongo na unafiki. Dhamiri zao zitabadilishwa.
3 Watawazuia kuoa na kupokea vyakula ambavyo Mungu aliviumba vitumiwe kwa
shukrani miongoni mwao waaminio na wenye kuijua kweli. 4 Kwa sababu kila
kitu ambacho Mungu amekiumba ni chema. Hakuna ambacho tunapokea kwa
shukrani kinastahili kukataliwa. 5 Kwa sababu kinatakaswa kupitia neno la Mungu
na kwa njia ya maombi. 6 Kama utayaweka mambo haya mbele ya ndugu, utakuwa
mtumishi mzuri wa Yesu Kristo. Kwa sababu umestawishwa kwa maneno ya imani
na kwa mafundisho mazuri ambayo umeyafuata. 7 Lakini zikatae hadithi za kidunia
ambazo zinapendwa na wanawake wazee. Badala yake, jifunze mwenyewe katika

utaua. [8] Kwa maana mazoezi ya mwili yafaa kidogo, bali utauwa wafaa sana kwa
mambo yote. Hutunza ahadi kwa maisha ya sasa na yale yajayo. [9] Ujumbe huu
ni wakuaminiwa na unastahili kukubaliwa kabisa. [10] Kwa kuwa ni kwa sababu
hii tunataabika na kufanya kazi kwa bidii sana. Kwa kuwa tunao ujasiri katika
Mungu aliye hai, ambaye ni Mwokozi wa watu wote, lakini hasa kwa waaminio.
[11] Uyaseme na kuyafundisha mambo haya. [12] Mtu yeyote asiudharau ujana wako.
Badala yake, uwe mfano kwa wote waaminio, katika usemi, mwenendo, upendo,
uaminifu, na usafi. [13] Mpaka nitakapokuja, dumu katika kusoma, katika kuonya, na
katika kufundisha. [14] Usiipuuze karama iliyomo ndani yako, ambayo ulipewa kupitia
unabii, kwa kuwekewa mikono na wazee. [15] Uyajali mambo haya. Ishi katika hayo
ili kukua kwako kuwe dhahiri kwa watu wote. Zingatia sana mwenendo wako na
mafundisho. [16] Dumu katika mambo haya. Maana kwa kufanya hivyo utajiokoa
mwenyewe na wale wanaokusikiliza.

# 5

[1] Usimkemee mwanamume mzee. Bali mtiye moyo kama baba yako. Uwatiye
moyo vijana wa kiume kana kwamba ni ndugu zako. [2] Uwatiye moyo wanawake
wazee kama mama zako, na wanawake vijana kama dada zako kwa usafi wote.
[3] Waheshimu wajane, wale walio wajane kweli kweli. [4] Lakini kama mjane ana
watoto au wajukuu, waache kwanza wajifunze kuonesha heshima kwa watu wa
nyumbani mwao wenyewe. Waache wawalipe wazazi wao mema, kwa kuwa hii
inapendeza mbele za Mungu. [5] Lakini mjane kweli kweli ni yule aliyeachwa peke
yake. Naye huweka tegemeo lake kwa Mungu. Siku zote hudumu katika sala
na maombi usiku na mchana. [6] Hata hivyo, mwanamke yule aishiye kwa anasa
amekufa, ingawaje yu hai. [7] Na uyahubiri haya mambo ili kwamba wasiwe na
lawama. [8] Ila kama mtu asipowatunza ndugu zake, hususani wale walioko nyumbani
mwake, ameikana imani na ni mmbaya kuliko mtu asiye amini. [9] Basi mwanamke
aandikishwe kwenye orodha kama mjane akiwa na umri usiopungua miaka sitini,
na ni mke wa mume mmoja. [10] Lazima awe amejulikana kwa matendo mema, ikiwa
ni kwamba amewajali watoto, au ameshakuwa mkarimu kwa wageni, au ameosha
miguu ya waaminio, au alimesaidia ambao wamekuwa wakiteswa, au alijitoa kwa
kazi yeyote njema. [11] Lakini kwa wale wajane vijana, kataa kuwaandikisha kwenye
orodha ya wajane. Kwa kuwa wakiingia kwenye matamanio ya kimwili dhidi ya
Kristo, wanataka kuolewa. [12] Kwa njia hii huingia kwenye hatia kwa kuwa huvunja
kujitoa kwao kwa awali. [13] Na pia huingia kwenye mazoea ya uvivu. Wao huzunguka
nyumba kwa nyumba. Si tu kwamba ni wavivu, bali pia huwa wasengenyaji na na
wenye kuingilia mambo ya wengine. Wao husema mambo wasiyopaswa kuyasema.
[14] Kwa hiyo mimi nataka wanawake vijana waolewe, wazae watoto, wasimamie
nyumba zao, ili kutokumpa adui nafasi ya kutushitaki kwa kufanya dhambi. [15] Kwa
sababu baadhi yao wameshamgeukia Shetani. [16] Kama mwanamke yeyote aaminiye
ana wajane, basi na awasaidie, ili kanisa lisilemewe, ili liweze kuwasaidia wale
walio wajane kweli kweli. [17] Basi wazee wale watawalao vyema wahesabiwe kuwa
wamestahili heshima maradufu, hasa wale wanaojishughulisha na kufundisha neno
la Mungu. [18] Kwa kuwa maandiko yanasema, “Usimfumbe ng'ombe kinywa apulapo
nafaka,” na “Mfanya kazi anastahili mshahara wake.” [19] Usipokee mashitaka dhidi
ya mzee isipokuwa kuna mashahidi wawili au watatu. [20] Waonye wakosaji mbele
ya watu wote ili wengine waliobaki labda wataogopa. [21] Nakuagiza kwa dhati
mbele ya Mungu, na mbele ya Kristo Yesu, na malaika wateule, kwamba uzitunze
maagizo haya bila ubaguzi wowote, na kwamba usifanye jambo lolote kwa upendeleo.
[22] Usimwekee mtu yeyote mikono haraka. Usishiriki dhambi ya mtu mwingine.

Yakupasa kujitunza mwenyewe uwe usafi. 23 Hakupasi kunywa maji pekee. Badala
yake, unywe mvinyo kidogo kwa ajili ya tumbo na magonjwa yako ya mara kwa mara.
24 Dhambi za baadhi ya watu hujulikana kwa uwazi, na huwatangulia hukumuni.
Lakini baadhi ya dhambi hufuata baadaye. 25 Vivyo hivyo, baadhi ya kazi njema
hujulikana kwa uwazi, lakini hata zingine hazitafichika.

# 6

1 Wale wote walio chini ya nira kama watumwa wawachukulie mabwana zao
kama wenye heshima zote, wanatakiwa kufanya hivyo ili jina la Mungu na
mafundisho yasitukanwe. 2 Watumwa wenye mabwana waaminio wasiwadharau
kwa sababu wao ni ndugu. Badala yake, wawatumikie zaidi. Kwa sababu mabwana
wanaosaidiwa kazi zao ni waamini na wanapendwa. Fundisha na kuyatangaza
mambo haya. 3 Iwapo mtu fulani anafundisha kwa upotovu na hayapokei maelekezo
yetu yenye kuaminika, ambayo ni maneno ya Bwana wetu Yesu Kristo, iwapo
hawalikubali fundisho liongozalo kwenye utauwa. 4 Mtu huyo anajivuna na hajui
chochote. Badala yake, ana vurugu na mabishano juu ya maneno. Maneno haya
huzaa wivu, ugomvi, matukano, shuku mbaya, 5 na vurugu za mara kwa mara
kati ya watu wenye akili zilizoharibika. Wanaiacha kweli. Wanafikiri kwamba
utauwa ni njia ya kuwa matajiri" 6 Sasa utauwa na kuridhika ni faida kubwa. 7 Kwa
maana hatukuja na chochote duniani. Wala hatuwezi kuchukua chochote kutoka
duniani. 8 Badala yake, tutosheke na chakula na mavazi. 9 Sasa hao watakao kuwa
na mali huanguka katika majaribu, katika mtego. Huanguka katika upumbavu
mwingi na tamaa mbaya, na katika kitu chochote kinachowafanya watu wazame
katika maangamizi na uharibifu. 10 Kwa kuwa kupenda fedha ni chanzo cha aina
zote za uovu. Watu ambao hutamani hiyo, wamepotoshwa mbali na imani na
wamejichoma wenyewe kwa huzuni nyingi. 11 Lakini wewe mtu wa Mungu, yakimbie
mambo hayo. Fuata haki, utauwa, uaminifu, upendo, usitahimilivu, na upole.
12 Piga vita vizuri vya imani. Shikilia uzima wa milele ulioitiwa. Ilikuwa ni kwa
sababu hii kwamba ulitoa ushuhuda mbele ya mashahidi wengi kwa kile kilicho
chema. 13 Nakupa amri hii mbele za Mungu, anayesababisha vitu vyote kuishi,
na mbele ya Yesu Kristo, aliyenena iliyo kweli kwa Pontio Pilato: 14 itunze amri
kwa ukamilifu, pasipo mashaka, hadi ujio wa Bwana wetu Yesu Kristo. 15 Mungu
atadhihirisha ujio wake kwa wakati sahihi- Mungu, Mbarikiwa, nguvu pekee, Mfalme
anayetawala, Bwana anayeongoza. 16 Peke yake anaishi milele na akaaye katika
mwanga usiokaribiriwa. Hakuna mtu awezaye kumwona wala awezaye kumtazama.
Kwake iwe heshima na uweza wa milele. Amina. 17 Waambie matajiri katika
ulimwengu huu wasijivune, na wasitumaini katika utajiri, ambao siyo wa uhakika.
Badala yake, wanapaswa kumtumaini Mungu. Ambaye hutupatia utajiri wote wa
kweli ili tufurahie. 18 Waambie watende mema, watajirike katika kazi njema, wawe
wakarimu, na utayari wa kutoa. 19 Katika njia hiyo watajiwekea msingi mzuri kwa
mambo yajayo, ili kwamba waweze kushika maisha halisi. 20 Timotheo, linda kile
ulichopewa. Jiepushe na majadiliano ya kipumbavu na mabishano yenye kujipinga
ambayo kwa kwa uongo huitwamaarifa. 21 Baadhi ya watu huyatangaza mambo
haya, na hivyo wameikosa imani. Neema na iwe pamoja nawe.

# 2 Timotheo

1 Paulo mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu, sawasawa na ahadi ya
uzima ulio ndani ya Kristo Yesu, 2 kwa Timotheo mwana mpendwa: Neema, rehema
na amani toka kwa Mungu Baba na Kristo Yesu Bwana wetu. 3 Ninamshukuru
Mungu, ambaye ninamtumikia kwa nia njema kama walivyofanya baba zangu,
ninapokumbuka daima katika maombi yangu. Usiku na 4 mchana ninatamani
kukuona, ili kwamba nijawe na furaha. Ninayakumbuka machozi yako. 5 Nimekuwa
nikikumbushwa kuhusu imani yako halisi, ambayo hapo kwanza ilikaa kwa bibi yako
Loisi na mama yako Yunisi. Na nina hakika ya kwamba imani hiyo inakaa ndani
yako pia. 6 Hii ndiyo sababu nakukumbusha kuchochea karama ya Mungu iliyomo
ndani yako kwa njia ya kuwekewa mikono yangu. 7 Kwa kuwa Mungu hakutupa
roho ya woga, bali ya nguvu na upendo na nidhamu. 8 Kwa hiyo usiuonee haya
ushuhuda kuhusu Bwana wetu, wala wangu mimi Paulo mfungwa wake. Bali ushiriki
mateso kwa ajili ya injili sawasawa na uweza wa Mungu. 9 Ni Mungu aliyetuokoa na
kutuita kwa wito mtakatifu. Hakufanya hivi kulingana na kazi zetu bali kulingana
na neema na mpango wake mwenyewe. Alitupatia mambo haya katika Kristo Yesu
kabla ya nyakati kuanza. 10 Lakini sasa wokovu wa Mungu umekwishafunuliwa kwa
kuja kwa mwokozi wetu Kristo Yesu. Ni Kristo aliyeikomesha mauti na kuleta uzima
usiokoma kwa nuru ya injili. 11 Kwa sababu hiyo nilichaguliwa kuwa mhubiri, mtume
na mwalimu. 12 Kwa sababu hii nateseka pia, lakini sioni haya kwa kuwa namjua
yeye niliyekwisha kumuamini. Nina hakika kuwa yeye anaweza kukitunza kile
nilichokikabidhi kwake hata siku ile. 13 Ukumbuke mfano wa ujumbe wa uaminifu
uliousikia toka kwangu, pamoja na imani na upendo ulio ndani ya Kristo Yesu.
14 Yatunze Mambo mazuri aliyokukabidhi Mungu kupitia Roho Mtakatifu aishiye
ndani yetu. 15 Unajua ya kuwa, wote waishio katika Asia waliniacha. Kwenye kundi
hili wamo Figelo na Hemogene. 16 Bwana airehemu nyumba ya Onesiforo kwa kuwa
mara nyingi aliniburudisha na hakuionea aibu minyororo yangu. 17 Badala yake,
alipokuwa Roma alinitafuta kwa bidii na akanipata. 18 Mungu amjalie kupata rehema
kutoka kwake siku ile. Kama alivyonisaidia nilipokuwa Efeso, wewe wajua vyema.

## 2

1 Kwa hiyo, wewe mwanangu, utiwe nguvu katika neema iliyondani ya Kristo
Yesu. 2 Na mambo uliyoyasikia kwangu miongoni mwa mashahidi wengi, uyakabidhi
kwa watu waaminifu ambao wataweza kuwafundisha wengine pia. 3 Shiriki mateso
pamoja nami, kama askari mwema wa Kristo Yesu. 4 Hakuna askari atumikae wakati
huo huo akijihusisha na shughuli za kawaida za maisha haya, ili kwamba ampendeze
ofisa wake mkuu. 5 Pia kama mtu akishindana kama mwanariadha, hatapewa taji
asiposhindana kwa kufuata kanuni. 6 Ni Muhimu kwamba mkulima mwenye bidii
awe wa kwanza kupokea mgao wa mazao yake. 7 Tafakari kuhusu nisemacho,
kwa maana Bwana atakupa uelewa katika mambo yote. 8 Mkumbuke Yesu Kristo,
kutoka uzao wa Daudi, ambaye alifufuliwa kutoka kwa wafu. Hii ni kulingana na
ujumbe wangu wa Injili, 9 ambao kwa sababu ya huo ninateswa hata kufungwa
minyororo kama mhalifu. Lakini neno la Mungu halifungwi kwa minyororo. 10 Kwa
hiyo, navumilia mambo yote kwa ajili ya wale ambao Mungu amekwishawachagua,
ili kwamba nao pia waupate wokovu ulio katika Kristo Yesu pamoja na utukufu
wa milele. 11 Usemi huu ni wakuaminika: “Ikiwa tumekufa pamoja naye, tutaishi
pamoja naye pia, 12 kama tukivumilia, tutatawala pamoja naye pia, kama tukimkana

yeye, naye pia atatukana sisi. 13 kama hatutakuwa waaminifu, yeye atabaki kuwa
mwaminifu, maana hawezi kujikana mwenyewe." 14 Endelea kuwakumbusha juu ya
mambo haya. Waonye mbele za Mungu waache kubishana kuhusu maneno. Kwa
sababu hakuna manufaa katika jambo hili. Kutokana na hili kuna uharibifu kwa
wale wanaosikiliza. 15 Fanya bidii kujionesha kuwa umekubalika kwa Mungu kama
mtenda kazi asiye na sababu ya kulaumiwa. Litumie neno la kweli kwa usahihi.
16 Jiepushe na majadiliano ya kidunia, ambayo huongoza kwa zaidi na zaidi ya uasi.
17 Majadiliano yao yatasambaa kama donda ndugu. Miongoni mwao ni Himenayo
na Fileto. 18 Hawa ni watu walioukosa ukweli. Wanasema ya kuwa ufufuo tayari
umishatokea. Wanapindua imani ya baadhi ya watu. 19 Hata hivyo, msingi imara
wa Mungu unasimama, wenye uandishi huu, "Bwana anawajua walio wake, na kila
alitajaye jina la Bwana ni lazima ajitenge na udhalimu." 20 Kwenye nyumba ya
kitajiri, siyo kwamba vimo vyombo vya dhahabu na shaba tu. Pia kuna vyombo
vya miti na udongo. Baadhi ya hivi ni kwa ajili ya matumizi ya heshima na baadhi
yake ni kwa matumizi yasiyo ya heshima. 21 Ikiwa mtu atajitakasa mwenyewe
kutoka kwenye matumizi yasiyo ya heshima, yeye ni chombo chenye kuheshimika.
Ametengwa maalumu, mwenye manufaa kwa Bwana, na ameandaliwa kwa kila kazi
njema. 22 Zikimbie tamaa za ujanani. Ukifuata haki, imani, upendo na amani pamoja
na wale wamwitao Bwana kwa moyo safi. 23 Lakini ukatae upumbavu na maswali
ya kipuuzi. Kwani unajua ya kuwa huzaa ugomvi. 24 Mtumishi wa Bwana hapaswi
kugombana, badala yake inampasa kuwa mpole kwa watu wote, awezaye kufundisha,
na mvumilivu. 25 Ni lazima awaelimishe kwa upole wale wampingao. Yamkini
Mungu aweze kuwapatia toba kwa kuifahamu kweli. 26 Waweze kupata ufahamu
tena na kuepuka mtego wa Shetani, baada ya kuwa wametekwa na yeye kwa ajili ya
mapenzi yake.

# 3

1 Lakini fahamu hili: katika siku za mwisho kutakuwa na nyakati ngumu. 2 kwa
sababu watu watakuwa wenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye
kujisifu, wenye majivuno, wenye dhihaka, wasiotii wazazi wao, wasiokuwa na
shukurani na waovu. 3 Wasio na upendo wa asili, wasiotaka kuishi kwa amani na
yeyote, wachonganishi, wasingiziaji, wasioweza kujizuia, wenye vurugu, wasiopenda
mema. 4 Watakuwa wasaliti, wakaidi, wenye kujipenda wenyewe na wapenda
anasa kuliko kumpenda Mungu. 5 Kwa nje watakuwa na sura ya ucha Mungu,
lakini wataikana nguvu yake. Jiepushe na watu hao. 6 Kwa kuwa baadhi yao ni
wanaume wanaoingia kwenye familia za watu na kushawishi wanawake wajinga.
Hawa ni wanawake waliojawa dhambi na wenye kuongozwa na tamaa za kila aina.
7 Wanawake hawa hujifunza siku zote, lakini kamwe hawawezi kuufikia ufahamu
wa ile kweli. 8 Kama vile ambavyo Yane na Yambre walisimama kinyume na
Musa. Kwa njia hii walimu hawa wa uongo husimama kinyume na kweli. Ni
watu walioharibiwa katika fikira zao, wasiokubalika kuhusiana na imani. 9 Lakini
hawataendelea mbali. Kwa kuwa upumbavu wao utawekwa wazi kwa watu wote,
kama ulivyokuwa wa wale watu. 10 Lakini wewe umeyafuata mafundisho yangu,
mwenendo wangu, makusudi yangu, imani yangu, uvumilivu wangu, upendo wangu
na ustahimilivu wangu, 11 mateso, maumivu na yaliyonipata kule Antiokia, Ikonio na
Listra. Niliyavumilia mateso. Bwana aliniokoa katika yote hayo. 12 Wote wanaotaka
kuishi katika maisha ya kumcha Mungu katika Kristo Yesu watateswa. 13 Watu
waovu na wadanganyifu watazidi kuwa waovu zaidi. Watawapotosha wengine. Wao
wenyewe wamepotoshwa. 14 Lakini wewe, dumu katika mambo uliyojifunza na
kuyaamini kwa uthabiti. Kwa kuwa unajua umejifunza kwa nani. 15 Unatambua

ya kuwa tangu utotoni mwako uliyajua maandiko matakatifu. Haya yanaweza
kukuhekimisha kwa ajili ya wokovu kwa njia ya imani katika kristo Yesu.
16 Kila andiko limetiwa pumzi na Mungu. Linafaa kwa mafundisho yenye faida, kwa
kushawishi, kwa kurekebisha makosa, na kwa kufundishia katika haki.
17 Hii ni kwamba mtu wa Mungu awe kamili, akiwa amepewa nyenzo zote kwa ajili ya
kutenda kila kazi njema.

# 4

1 Ninakupa agizo hili lenye uzito mbele za Mungu na Kristo Yesu, atakaye
wahukumu walio hai na wafu, na kwa sababu ya kufunuliwa kwake na Ufalme wake:
2 Hubiri Neno. Uwe tayari kwa wakati ufaao na usiofaa. Waambie watu dhambi zao,
kemea, himiza, kwa uvumilivu wote na mafundisho.
3 Kwa maana wakati utakuja
ambao watu hawatachukuliana na mafundisho ya kweli. Badala yake, watajitafutia
walimu wa kufundisha kulingana na tamaa zao. kwa njia hii masikio yao yatakuwa
yametekenywa.
4 Wataacha kusikiliza mafundisho ya kweli, na kugeukia hadithi.
5 Lakini wewe uwe mwaminifu katika mambo yote, vumilia magumu, fanya kazi ya
mwinjilisti; timiza huduma yako.
6 Kwa maana mimi tayari nimekwisha kumiminwa.
Muda wa kuondoka kwangu umewadia.
7 Nimeshindana katika haki, Mwendo
nimeumaliza, Imani nimeilinda.
8 Taji ya haki imewekwa kwa ajili yangu, ambayo
Bwana, anayehukumu kwa haki, atanipa siku ile. Na siyo kwangu tu bali pia kwa
wote wanaongojea kwa shauku kuonekana kwake.
9 Jitahidi kuja kwagu haraka.
10 Kwa kuwa Dema ameniacha. Anaupenda ulimwengu wa sasa na amekwenda
Thesalonike, Kreseni alikwenda Galatia, na Tito alikwenda Dalmatia.
11 Luka tu
ndiye yuko pamoja nami. Umchukue Marko uje naye kwani yeye ni muhimu kwangu
katika huduma.
12 Nimemtuma Tikiko Efeso.
13 Lile joho ambalo nililiacha Troa kwa
Karpo, utakapokuja lilete, pamoja na vile vitabu hasa vile vya ngozi.
14 Alekizanda
mfua chuma alinitendea maovu mengi. Bwana atamlipa kulingana na matendo yake.
15 Nawe pia jihadhari naye, kwani aliyapinga sana maneno yetu.
16 Katika utetezi
wangu wa kwanza, hakuna mtu yeyote aliyesimama pamoja nami, badala yake, kila
mmoja aliniacha. Mungu asiwahesabie hatia.
17 Lakini Bwana alisimama pamoja
nami, akanitia nguvu ili kwamba kupitia kwangu, neno linenwe kwa ukamilifu na
mataifa wapate kusikia. Niliokolewa katika kinywa cha Simba.
18 Bwana ataniepusha
na matendo yote maovu na kuniokoa kwa ajili ya ufalme wake wa mbinguni. Utukufu
uwe kwake milele na milele. Amen
19 Msalimie Priska, Akila na nyumba ya Onesiforo.
20 Erasto alibaki huko Korintho, lakini Trifimo nilimuacha Mileto akiwa mgonjwa.
21 Fanya hima uje kabla ya kipindi cha baridi. Eubulo anakusalimu, pia Pude, Lino,
Claudia na ndugu wote.
22 Mungu awe pamoja na roho yako, Neema iwe nawe.

# Tito

1 Paulo, mtumishi wa Mungu na mtume wa Yesu Kristo, kwa imani ya wateule
wa Mungu na maarifa ya kweli iletayo utauwa. 2 Wapo katika tumaini la uzima wa
milele ambao Mungu asiyeweza kusema uongo aliuahidi tangu milele. 3 Kwa wakati
muafaka, alilifunua neno lake katika ujumbe alionipa mimi kuhubiri. Ilinipasa
kufanya hivi kwa amri ya Mungu mwokozi wetu. 4 Kwa Tito, mwana wa kweli
katika imani yetu. Neema, huruma na amani kutoka kwa Mungu Baba na Yesu Kristo
mwokozi wetu. 5 Kwa sababu hii nalikuacha Krete, kwamba uyatengeneze mambo
yote yaliyokuwa hayajakamilika na kuweka wazee wa kanisa kwa kila mji kama
nilivyokuagiza. 6 Mzee wa kanisa lazima asiwe na lawama, mme wa mke mmoja,
aliye na watoto waaminifu wasioshuhudiwa mabaya au wasio na nidhamu. 7 Ni
muhimu kwa mwangalizi, kama msimamizi wa nyumba ya Mungu, asiwe na lawama.
Asiwe mtu wa kelele au asiye jizuia. Lazima asiwe mwepesi wa hasira, asiwe mlevi,
asiwe mtu wa kusababisha ugomvi, na asiwe mwenye tamaa. 8 Badala yake: awe
mtu mkaribishaji, apendaye wema. Lazima awe mtu mwenye akili timamu, mwenye
haki, mcha Mungu, anayejitawala mwenyewe. 9 Awezaye kusimamia mafundisho ya
kweli yaliyofundishwa, ili aweze kuwatia moyo kwa mafundisho mazuri na awezaye
kuwarekebisha wote wanaompinga. 10 Kwa kuwa kuna waasi wengi, hasa wale wa
tohara. Maneno yao ni ya upuuzi. Wanadanganya na kuwaongoza watu katika
upotovu. 11 Ni lazima kuwazuia watu kama hao. Wanafundisha yale wasiyopaswa
kwa faida za aibu na kuharibu familia zote. 12 Mmoja wao, mtu mwenye busara,
alisema, “Wakrete wana uongo usio na mwisho, wabaya na wanyama wa hatari,
wavivu na walafi.” 13 Haya maelezo ni ya kweli, kwa hiyo uwazuie kwa nguvu ili
kwamba waweze kusema kweli katika imani. 14 Wewe usijihusishe na hadithi zisizo
za kweli za Kiyahudi au amri za watu, ambao hurudisha nyuma ukweli. 15 Kwa wote
walio safi, vitu vyote ni visafi. Lakini kwa wote walio wachafu na wasioamini, hakuna
kilicho kisafi. Kwa kuwa mawazo yao na dhamira zao zimechafuliwa. 16 Wanakiri
kumjua Mungu, lakini kwa matendo yao wanamkana. Wao ni waovu na wasiotii.
Hawakuthibitishwa kwa tendo lolote jema.

## 2

1 Lakini wewe yaseme yale yanayoendana na maelekezo ya kuaminika. 2 Wazee
wawe na kiasi, heshima, busara, imani safi, katika upendo, na katika uvumilivu.
3 Vilevile wanawake wazee lazima daima wajioneshe wao wenyewe kama wenye ku-
jiheshimu, na sio wasengenyaji. Lazima wasiwe watumwa wa pombe. 4 Wanapaswa
kufundisha yaliyo mazuri ili kuwaandaa wasichana kwa busara kuwapenda waume
zao na watoto wao. 5 Wanapaswa kuwafundisha kuwa na busara, wasafi, watunzaji
wazuri wa nyumba zao, na watii kwa waume zao wenyewe. Inawalazimu kufanya
mambo haya ili kwamba neno la Mungu lisitukanwe. 6 katika namna iyo hiyo, watieni
moyo vijana wa kiume wawe na busara. 7 Katika njia zote jiwekeni wenyewe kuwa
mfano katika kazi nzuri; na mfundishapo, onesheni uadilifu na heshima. 8 Ongeeni
ujumbe wenye afya na usio na dosari, ili kwamba yeyote apingaye aaibishwe kwa
sababu hana baya la kusema juu yetu. 9 Watumwa na wawatii mabwana zao katika
kila kitu. Wanapaswa kuwafurahisha na sio kubishana nao. 10 Hawapaswi kuiba.
Badala yake, wanapaswa kuonesha imani yote nzuri ili kwamba katika njia zote
wayapambe mafundisho yetu kumhusu Mungu mwokozi wetu. 11 Kwa kuwa neema
ya Mungu imeonekana kwa watu wote. 12 Inatufundisha kukataa mambo yasiyo

ya kimungu na tamaa za kidunia. Inatufundisha kuishi kwa busara, kwa haki, na
katika njia za kimungu kwa wakati huu. [13] Wakati tunatarajia kupokea tumaini letu
lenye baraka, mwonekano wa utukufu wa Mungu wetu mkuu na Mwokozi wetu Yesu
Kristo. [14] Yesu alijitoa mwenyewe kwa ajili yetu ili kutukomboa kutoka katika uasi
na kutufanya wasafi, kwa ajili yake, watu maalumu walio na hamu ya kufanya kazi
nzuri. [15] Yaseme na kuyasisitiza mambo haya. Kemea kwa mamlaka yote. Usikubali
mtu yeyote akupuuze.

# 3

[1] Uwakumbushe kuwanyenyekea viongozi na mamlaka, kuwatii na kuwa tayari
katika kila kazi njema. [2] Wakumbushe kutokumtendea mtu yeyote ubaya, waepuke
majibizano, wawape nafasi watu wengine katika kufanya maamuzi, na kuonesha
unyenyekevu kwa watu wote. [3] Kwa kuwa sisi pia tulikuwa na mawazo potofu na
wakaidi. Tulikuwa upotevuni na tulifanywa watumwa kwa tamaa nyingi na starehe.
Tuliishi katika wivu na uovu. Tulichukiza na kuchukiana. [4] Lakini wakati huruma
ya Mungu mwokozi wetu na upendo wake kwa wanadamu ulipoonekana, [5] haikuwa
kwa matendo yetu ya haki tuliyofanya, bali alituokoa kwa neema yake. Alituokoa
kwa kutuosha kwa kuzaliwa upya na katika kufanywa upya kwa Roho Mtakatifu.
[6] Mungu alimwaga Roho Mtakatifu kwa wingi juu yetu kupitia Yesu Kristo mwokozi
wetu. [7] Alifanya hivi ili kwamba, tukiwa tumehesabiwa haki kwa neema yake, tuwe
washirika katika uhakika wa maisha ya milele. [8] Huu ni ujumbe wa kuaminika.
Ninawataka myanene kwa ujasiri mambo haya, ili kwamba wale wanaomwamini
Mungu wawe na dhamira juu ya kazi nzuri ambayo aliiweka mbele yao. Mambo haya
ni mazuri na yanafaida kwa ajili ya watu wote. [9] Lakini jiepusheni na mijadala ya
kipumbavu, nasaba, mashindano, na migongano kuhusu sheria. Mambo hayo hayana
maana wala faida. [10] Mkataeni yeyote anayesababisha migawanyiko kati yenu. Baada
ya onyo moja ama mawili, [11] jueni kwamba mtu wa jinsi hiyo ameiacha njia iliyo
sahihi na anatenda dhambi na kujihukumu mwenyewe. [12] Nitakapomtuma kwako
Artemi au Tikiko, harakisha uje kwangu huku Nikopoli ambapo nimeamua kukaa
kipindi cha baridi. [13] Harakisha na umtume Zena mtaalamu katika sheria, na Apolo,
pasipo kupungukiwa na kitu. [14] Watu wetu lazima wajifunze kujishughulisha katika
kazi nzuri ambazo zinagusa mahitaji muhimu ili kwamba wasije wakawa wasiozaa
matunda. [15] Wote walio pamoja nami wanakusalimu. Wasalimu wale watupendao
katika imani. Neema iwe nanyi nyote.

# Filemoni

1 Paulo, mfungwa wa Kristo Yesu, na ndugu Timotheo kwa Filemoni, mpendwa
rafiki yetu na mtenda kazi pamoja nasi, 2 na kwa Afia dada yetu, na kwa Arkipas
askari mwenzetu, na kwa kanisa lile linalokutana nyumbani kwako. 3 Neema iwe
kwenu na amani itokayo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana Yesu Kristo. 4 Wakati
wote namshukuru Mungu. Ninakutaja katika maombi yangu. 5 Nimesikia upendo
na imani uliyonayo katika Bwana Yesu na kwa ajili ya waumini wote. 6 Ninaomba
kwamba ushirika wa imani yenu iwe na ufanisi katika ujuzi wa kila jambo jema
lililoko kati yetu katika Kristo. 7 Kwa kuwa nimekuwa na furaha na faraja kwa sababu
ya upendo wako, kwa sababu mioyo ya waumini imekuwa ikitulizwa nawe, ndugu.
8 Kwa hiyo, ingawa nina ujasiri wote katika Kristo kukuamuru wewe kufanya kile
unachoweza kufanya, 9 lakini kwa sababu ya upendo, badala yake nakusihi - mimi,
Paulo niliye mzee, na sasa ni mfungwa kwa ajili ya Kristo Yesu. 10 Ninakusihi kuhusu
mwanangu Onesmo, niliyemzaa katika vifungo vyangu. 11 Kwa kuwa mwanzoni
hakukufaa, lakini sasa anakufaa wewe na mimi. 12 Nimemtuma- yeye ambaye ni wa
moyo wangu hasa - kurudi kwako. 13 Nataraji angeendelea kubaki pamoja nami, ili
anitumikie badala yako, wakati niwako kifungoni kwa ajili ya injili. 14 Lakini sikutaka
kufanya jambo lolote bila ruhusa yako. Nilifanya hivi ili kwamba jambo lolote
zuri lisifanyike kwa sababu nilikulazimisha, bali kwa sababu ulipenda mwenyewe
kulitenda. 15 Labda ni sababu alitengwa nawe kwa muda, ilikuwa hivyo ili uwe
pamoja naye milele. 16 Ili kwamba asiwe tena mtumwa, bali bora zaidi ya mtumwa,
kama ndugu mpendwa, hasa kwangu, na zaidi sana kwako, katika mwili na katika
Bwana. 17 Na hivyo kama wanichukulia mimi mshirika, mpokee kama ambavyo
ungenipokea mimi. 18 Lakini kama amekukosea jambo lolote, au unamdai kitu
chochote, kidai hicho kutoka kwangu. 19 Mimi Paulo, ninaandika kwa mkono wangu
mwenyewe: mimi nitakulipa. Sisemi kwako kwamba nakudai maisha yako hasa.
20 Naam ndugu, acha nipate furaha ya Bwana toka kwako: uburudishe moyo wangu
katika Kristo. 21 Nikiwa na imani kuhusu utii wako, nakuandikia nikijua kwamba
utafanya hata zaidi ya vile ninavyokuomba. 22 Wakati huo huo andaa chumba cha
wageni kwa ajili yangu, kwa kuwa ninatumaini kupitia maombi yako nitakutembelea
hivi karibuni. 23 Epafra, mfungwa mwenzangu katika Kristo Yesu anakusalimu, 24 na
kama afanyavyo Marko, Aristarko, Dema, Luka, watendakazi pamoja nami. 25 Neema
ya Bwana Yesu Kristo iwe pamoja na roho yako. Amina.

# Wahebrania

1 Nyakati zilizopita Mungu alizungumza na mababu zetu kupitia manabii mara
nyingi na kwa njia nyingi. 2 Lakini katika siku hizi tulizonazo, Mungu ameongea nasi
kupitia Mwana, ambaye alimweka kuwa mrithi wa vitu vyote, na ambaye kupitia
yeye pia aliumba ulimwengu. 3 Mwanawe ni nuru ya utukufu wake, tabia pekee
ya asili yake, na anayeendeleza vitu vyote kwa neno la nguvu zake. Baada ya
kukamilisha utakaso wa dhambi, aliketi chini mkono wa kulia wa enzi huko juu.
4 Amekuwa bora kuliko malaika, kama vile jina alilolirithi lilivyo bora zaidi kuliko
jina lao. 5 Kwa maana ni kwa malaika gani aliwahi kusema, “Wewe ni mwanangu,
leo nimekuwa baba yako?” Na tena, “Nitakuwa baba kwake, naye atakuwa mwana
kwangu?” 6 Tena, wakati Mungu alipomleta mzaliwa wa kwanza ulimwenguni,
husema, “Malaika wote wa Mungu lazima wamwabudu.” 7 Kuhusu malaika asema,
“Yeye ambaye hufanya malaika zake kuwa roho, na watumishi wake kuwa ndimi za
moto.” 8 Lakini kuhusu Mwana husema, “Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele
na milele. Fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya haki. 9 Umependa haki na kuchukia
uvunjaji wa sheria, kwa hiyo Mungu, Mungu wako, amekupaka mafuta ya furaha
kuliko wenzako.” 10 Hapo mwanzo, Bwana, uliweka msingi wa dunia. Mbingu ni
kazi za mikono yako. 11 Zitatoweka, lakini wewe utaendelea. Zote zitachakaa kama
vazi. 12 Utazikunjakunja kama koti, nazo zitabadilika kama vazi. Lakini wewe ni
yuleyule, na miaka yako haitakoma.” 13 Lakini ni kwa malaika yupi Mungu alisema
wakati wowote, “Keti mkono wangu wa kulia mpaka nitakapowafanya adui zako
kuwa kiti cha miguu yako”? 14 Je, malaika wote siyo roho zilizotumwa kuwahudumia
na kuwatunza wale watakaourithi wokovu?

## 2

1 Kwa hiyo ni lazima tuweke kipaumbele zaidi kwa yale tuliyosikia, ili kwamba
tusije tukatengwa mbali nayo. 2 Kwa maana ikiwa ujumbe uliozungumzwa na
malaika ni halali, na kila kosa na uasi hupokea adhabu tu, 3 tutapataje kuepuka kama
tusipojali wokovu huu mkuu? —wokuvu ambao kwanza ulitangazwa na Bwana na
kuthibitishwa kwetu na wale waliousikia. 4 Mungu pia aliuthibitisha kwa ishara,
maajabu, na kwa matendo makuu mbalimbali, na kwa zawadi za Roho Mtakatifu
alizozigawa kulingana na mapenzi yake mwenyewe. 5 Mungu hakuuweka ulimwengu
ujao, ambao tunaongelea habari zake, chini ya malaika. 6 Badala yake, mtu fulani
ameshuhudia mahali fulani akisema, “Mtu ni nani, hata uweze kumkumbuka? Au
mwana wa mtu, hata umtunze? 7 mtu kuwa mdogo kuliko malaika; umemvika taji ya
utukufu na heshima. (Zingatia: Katika nakala halisi za kwanza, mstari huu haupo.
“Na umemuweka juu ya kazi ya mikono yako.) 8 Umeweka kila kitu chini ya miguu
yake.” Kwa hiyo Mungu ameweka kila kitu chini ya mtu. Hakuacha kitu chochote
ambacho hakiko chini yake. Lakini sasa hivi hatuoni bado kila kitu kikiwa chini yake.
9 Hata hivyo, tunaona ambaye alikuwa amefanywa kwa muda, chini kuliko malaika—
Yesu, ambaye, kwa sababu ya mateso yake na kifo chake, amevikwa taji ya utukufu
na heshima. Hivyo sasa kwa neema ya Mungu, Yesu ameonja kifo kwa ajili ya kila
mtu. 10 Ilikuwa sahihi kwamba Mungu, kwa sababu kila kitu kipo kwa ajili yake na
kupitia yeye, alipaswa kuwaleta watoto wengi katika utukufu, na kwamba alipaswa
kumfanya kiongozi katika wokovu wao kuwa mkamilifu kupitia mateso yake. 11 Kwa
maana wote wawili yule anayeweka wakfu na wale ambao wanawekwa wakfu, wote
wanatoka kwenye asili moja, Mungu. Kwa sababu hii yule anayewaweka wakfu

kwa Mungu haoni aibu kuwaita ndugu. [12] Anasema, “Nitatangaza jina lako kwa
ndugu zangu, nitaimba kuhusu wewe kutoka ndani ya kusanyiko.” [13] Tena asema,
“Nitaamini katika yeye.” Na tena, “Tazama, hapa nipo na watoto ambao Mungu
amenipa.” [14] Kwa hiyo, kwa kuwa watoto wa Mungu wote hushiriki mwili na damu,
kadhalika Yesu alishiriki vitu vilevile, ili kwamba kupitia kifo apate kumdhohofisha
yule ambaye ana mamlaka juu ya mauti, ambaye ni ibilisi. [15] Hii ilikuwa hivyo ili
awaweke huru wale wote ambao kupitia hofu ya kifo waliishi maisha yao yote katika
utumwa. [16] Kwa hakika siyo malaika anaowasaidia. Badala yake, anawasaidia wazao
wa Abraham. [17] Kwa hiyo, ilikuwa lazima yeye awe kama ndugu zake katika njia zote,
ili aweze kuwa kuhani mkuu mwenye huruma na mwaminifu kwa vitu vya Mungu,
na ili kwamba awe na uwezo wa kutoa msamaha kwa dhambi za watu. [18] Kwa
sababu Yesu mwenyewe ameteseka, na kujaribiwa, ana uwezo wa kuwasaidia wale
wanaojaribiwa.

# 3

[1] Kwa hiyo, ndugu watakatifu, washiriki wa wito wa mbinguni, mumfikiri Yesu,
Mtume na Kuhani Mkuu wa ukiri wetu. [2] Alikuwa mwaminifu kwa Mungu
aliyemteua, kama Musa alivyokuwa mwaminifu pia katika nyumba yote ya Mungu.
[3] Kwa kuwa Yesu amehesabiwa kuwa na heshima kubwa kuliko aliyokuwa nayo
Musa, kwa sababu yule anayejenga nyumba anahesabiwa kuwa na heshima kubwa
kuliko nyumba yenyewe. [4] Kwa kuwa kila nyumba hujengwa na mtu fulani,
lakini yule anayejenga kila kitu ni Mungu. [5] Hakika Musa alikuwa mwaminifu
kama mtumishi katika nyumba yote ya Mungu, akitoa ushuhuda kuhusu mambo
yatakayosemwa wakati ujao. [6] Lakini Kristo ni Mwana katika usimamizi wa nyumba
ya Mungu. Sisi ni nyumba yake kama tutashikilia haraka katika kujiamini na fahari
ya kujiamini. [7] Kwa hiyo, ni kama Roho Mtakatifu asemavyo, “Leo, kama utasikia
sauti yake, [8] Usiufanye moyo wako kuwa mgumu kama Waisraeli walivyofanya katika
uasi, katika wakati wa kujaribiwa nyikani. [9] Huu ulikuwa wakati ambao baba
zenu waliniasi kwa kunijaribu, na wakati, kwa miaka arobaini, waliona matendo
yangu. [10] Kwa hiyo sikufurahishwa na kizazi hicho. Nilisema, 'Wanapotea kila mara
katika mioyo yao, na hawajui njia zangu. [11] Ni kama vile nilivyoapa katika hasira
yangu: hawataiingia raha yangu.” [12] Muwe waangalifu, ndugu, ili kwamba usije
ukawepo moyo mwovu wa kutokuamini kwa mmoja wenu, moyo ambao utakwenda
mbali na Mungu aliye hai. [13] Badala yake, mhamasishane kila siku kila mmoja
na mwenzie, ili kila iitwapo leo mtamani, ili kwamba mmoja kati yenu asifanywe
kuwa mgumu kwa udanganyifu wa dhambi. [14] Kwa maana tumekuwa washiriki wa
Kristo ikiwa tutashikamana na uthabiti wetu kwa nguvu katika yeye kutoka mwanzo
hadi mwisho. [15] Kuhusu hili imekwisha kusemwa, “Leo kama mtaisikiliza sauti
yake, msiifanye mioyo yenu kuwa migumu, kama Waisraeli walivyofanya wakati wa
uasi.” [16] Ni akina nani hao waliomsikia Mungu na kuasi? Hawakuwa wale wote
ambao Musa alikuwa amewaongoza kutoka Misri? [17] Na kina nani ambao Mungu
aliwakasirikia kwa miaka arobaini? Siyo pamoja na wale waliotenda dhambi, ambao
miili yao iliyokufa ililala jangwani? [18] Ni akina nani aliowaapia Mungu kwamba
hawataingia katika raha yake, kama siyo wale ambao hawakumtii yeye? [19] Tunaona
kwamba hawakuweza kuingia katika raha yake kwa sababu ya kutokuamini.

# 4

[1] Kwa hiyo, tunapaswa kuwa makini ili kwamba kati yenu asiwepo hata mmoja
atakayeonekana kushindwa kufikia ahadi endelevu ya kuingia katika pumzika
la Mungu. [2] Kwani tumekuwa na habari njema kuhusu pumziko la Mungu

lililotangazwa kwetu kama Waisrael walivyokuwa nayo, lakini ujumbe huo haukuwa-
saidia wale ambao waliusikia bila kuunganisha imani kwa hilo. 3 Kwa sisi, ambao
tumekwisha amini-sisi ndio miongoni tutakaoingia katika lile pumuziko, Kama
inavyosema, “Kama nilivyoapa kwa hasira yangu, Hawataingia katika pumziko
mwangu.” Alisema hili, ingawa kazi zote alizotengeneza zilikuwa zimekamilika tangu
mwanzo wa ulimwengu. 4 Kwani ameshasema sehemu fulani kuhusu siku ya saba,
“Mungu alipumzika siku ya saba katika yote aliyoyafanya.” 5 Tena ameshasema,
“Hawataingia kwenye pumziko langu.” 6 Kwa sababu hiyo, tangu pumziko la Mungu
bado ni akiba kwa ajili ya baadhi kuingia, na tangu Waisraeli wengi ambao walisikia
habari njema kuhusu pumziko lake hawakuingia kwa sababu ya kutotii, 7 Mungu
aliweka tena siku fulani, iitwayo “Leo.” Yeye aliiongeza siku hii alipozungumza
kupitia Daudi, ambaye alisema kwa muda mrefu baada ya yaliyosemwa kwanza,
“Leo kama mtasikia sauti yake, msifanye mioyo yenu kuwa migumu.” 8 Kwani kama
Yoshua aliwapatia pumziko, Mungu asingelisema juu ya siku nyingine. 9 Kwa hiyo
bado kuna Sabato ya pumziko iliyotunzwa kwa ajili ya watu wa Mungu. 10 Kwani
anayeingia katika pumziko la Mungu yeye mwenyewe pia amepumzika kutokana na
matendo yake, kama Mungu alivyofanya katika yeye. 11 Kwa hiyo tuweni na shauku
ya kuingia katika lile pumziko, ili kwamba asiwepo atakayeanguka katika aina ya
uasi waliofanya. 12 Kwa maana neno la Mungu li hai na lina nguvu na linaukali
kuliko upanga wowote wenye makali kuwili. Na huchoma hata kufikia kugawanya
nafsi na roho, na viungo kutika uboho. Na lenye kuweza kufahamu fikira za moyo
nia yake. 13 . Hakuna kilichoumbwa kilichojificha katika uso wa Mungu. Badala yake,
kila kitu ni dhahiri na wazi kwa macho ya mmoja ambaye ni lazima tutoe hesabu.
14 Baadaye kuwa na kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu Mwana wa Mungu,
kwa uimara tushikilie imani zetu. 15 Kwa kuwa hatuna kuhani mkuu ambaye hawezi
kuhisi huruma kwa ajili udhaifu wetu, lakini yeye ambaye kwa njia zote amekuwa
akijaribiwa kama sisi, isipokuwa yeye ambaye hana dhambi. 16 Na tuje kwa ujasiri
katika kiti cha enzi cha neema, ili kwamba tupokee rehema na kupata neema ya
kutusaidia wakati wa hitaji.

# 5

1 Kwani kila kuhani mkuu, aliyechaguliwa kutoka miongoni mwa watu, amechag-
uliwa kusimama badala yao katika vitu vinavyohusiana na Mungu, ili aweze kutoa
kwa pamoja zawadi na dhabihu kwa ajili ya dhambi. 2 Anaweza kujishughulisha
kwa upole na wajinga na wabishi kwa kuwa yeye mwenyewe pia amezungukwa na
udhaifu. 3 Kwa sababu ya hili, ana wajibu wa kutoa sadaka kwa ajili ya dhambi zake
kama afanyavyo kwa dhambi za watu. 4 Na hakuna mtu achukuaye heshima hii kwa
ajili yake mwenyewe, lakini badala yake, lazima aitwe na Mungu, kama alivyokuwa
Haruni. 5 Hata Kristo hakujipa heshimu mwenyewe kwa kujifanya mwenyewe
kuwa kuhani mkuu. Badala yake, Mungu alisema kwake, “ Wewe ni mwanangu,
leo nimekuwa Baba yako.” 6 Ni kama asemavyo pia sehemu nyingine, “ Wewe ni
kuhani milele baada ya mfumo wa Melkizedeki.” 7 Wakati wa kipindi chake katika
mwili, aliomba na kuombea, alimwomba Mungu kwa machozi, kwa yeye awezaye
kumwokoa kutoka kwenye kifo. Kwa sababu ya unyenyekevu wake kwa Mungu,
alisikiwa. 8 Ijapokuwa alikua mwana, alijifunza kutii kwa mambo yaliyomtesa.
9 Alikamilishwa na kwa njia hii alifanyika kwa kila mtu amwaminiye kuwa sababu
ya wokovu wa milele, 10 kwa kutengwa na Mungu kama kuhani Mkuu baada ya zamu
ya Melkizedeki. 11 Tuna mengi ya kusema kuhusu Yesu, lakini ni vigumu kuwaelezea
kwa kuwa ninyi ni wavivu wa kusikia. 12 Ijapokuwa kwa kipindi hiki mlipaswa kuwa
walimu, bado kuna umuhimu wa mtu kuwafundisha mafundisho ya awali ya kanuni

za neno la Mungu. Mnahitaji maziwa na si chakula kigumu. 13 Kwa kuwa yeyote
anywaye maziwa tu hana uzoefu katika ujumbe wa haki, kwa kuwa bado ni mtoto.
14 Kwa upande mwingine, chakula kigumu ni cha watu wazima, wale ambao kwa
sababu ya uzoefu wao katika kutofautisha haki na ubaya wamefundishwa kutambua
jema na ovu.

# 6

1 Kwa hiyo, tukiacha tulichojifunza kwanza kuhusu ujumbe wa Kristo, twapaswa
kuwa na juhudi kuelekea kwenye ukomavu, tusiweke tena misingi ya toba kutoka
katika kazi zisizo na uhai na imani katika Mungu, 2 wala misingi ya mafundisho
ya ubatizo, na kuwawekea mikono, ufufuo wa wafu, na hukumu ya milele. 3 Na
tutafanya hivi ikiwa Mungu ataruhusu. 4 Kwa kuwa haiwezekani kwa wale ambao
waliipata nuru awali, ambao walionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa kuwa
washirika wa Roho Mtakatifu, 5 na ambao walionja uzuri wa neno la Mungu na
kwa nguvu za wakati ujao, 6 na kisha wakaanguka - haiwezekani kuwarejesha
tena katika toba. Hii ni kwa sababu wamemsulubisha Mwana wa Mungu mara
ya pili kwa nafsi zao, wakimfanya kuwa chombo cha dhihaka hadharani. 7 Kwa
kuwa ardhi iliyopokea mvua inyeshayo mara kwa mara juu yake, na ikatoa mazao
muhimu kwa hao waliofanya kazi katika ardhi, hupokea baraka kutoka kwa Mungu.
8 Lakini ikiwa huzaa miiba na magugu, haina tena thamani na ipo katika hatari
ya kulaaniwa. Mwisho wake ni kuteketezwa. 9 Ijapokuwa tunazungumza hivi, rafiki
wapenzi, tunashawishiwa na mambo mazuri yawahusuyo ninyi na mambo yahusuyo
wokovu. 10 Kwa kuwa Mungu si dhalimu hata asahau kazi yenu na kwa upendo
mliouonesha kwa ajili ya jina lake, katika hili mliwatumikia waamini na bado mngali
mnawatumikia. 11 Na tunatamani sana kwamba kila mmoja wenu aweze kuonesha
bidii ile ile mpaka mwisho kwa uhakika wa ujasiri. 12 Hatutaki muwe wavivu,
lakini muwe wafuasi wa wale warithio ahadi kwa sababu ya imani na uvumilivu.
13 Kwa maana Mungu alipompa Abrahamu ahadi, aliapa kwa nafsi yake, kwa kuwa
asingeliapa kwa mwingine yeyote aliye mkubwa kuliko yeye. 14 Alisema, “Hakika
nitakubariki, na nitauongeza uzao wako zaidi.” 15 Kwa njia hii, Abrahamu alipokea
kile alichoahidiwa baada ya kusubiria kwa uvumilivu. 16 Maana wanadamu huapa
kwa yeye aliye mkuu kuliko wao, na kwao ukomo wa mashindano yote ni kiapo kwa
kuyathibitisha. 17 Wakati Mungu alipoamua kuonesha kwa uwazi zaidi kwa warithi
wa ahadi kusudi lake zuri lisilobadilika, alilithibitisha kwa kiapo. 18 Alifanya hivyo ili
kwa vitu viwili visivyoweza kubadilika, ambavyo katika hivyo Mungu hawezi kusema
uongo, sisi tulioikimbilia hifadhi tupate kutiwa moyo kushikilia kwa nguvu tumaini
lililowekwa mbele yetu. 19 Tunao ujasiri huu kama nanga imara na ya kutegemea ya
roho zetu, ujasiri ambao unaingia sehemu ya ndani nyuma ya pazia. 20 Yesu aliingia
sehemu ile kama mtangulizi wetu, akisha kufanyika kuhani mkuu hata milele baada
ya utaratibu wa Melkizedeki.

# 7

1 Ilikuwa hivi Melkizedeki, mfalme wa Salemu, Kuhani wa Mungu aliye juu, aliyeku-
tana na Abrahamu akirudi kutoka kuwaua wafalme na akambariki. 2 Abrahamu
alimpa moja ya kumi ya kila kitu alichokuwa amekiteka. Jina lake “Melkizedeki “
maana yake” mfalme wa haki” na pia “mflame wa Salemu” ambayo ni “mfalme wa
amani.” 3 Hana baba, hana mama, hana wazazi, hana mwanzo wa siku wala mwisho
wa maisha yake. Badala yake, anabakia kuhani milele, kama mwana wa Mungu.
4 Sasa fikiria jinsi huyu mtu alivyokuwa mkuu. Mzazi wetu Abrahamu alimpa moja ya
kumi ya vitu vizuri alivyovichukua vitani. 5 Na hakika, ukoo wa Walawi waliopokea

ofisi za kikuhani walikuwa na amri kutoka kwenye sheria kukusanya moja ya kumi
kutoka kwa watu, ambayo ni, kutoka kwa Wairaeli wenzao, pamoja na kwamba wao,
pia, ni ukoo kutoka kwa Abrahamu. 6 Lakini Melkizedeki, ambaye hakuwa wa ukoo
kutoka kwa Walawi, alipokea moja ya kumi kutoka kwa Abrahamu, na akambariki,
yeye aliyekuwa na ahadi. 7 Hapo haikataliwi kwamba mtu mdogo hubarikiwa na
mkubwa. 8 Kwa jambo hili mtu apokeaye moja ya kumi atakufa siku moja, lakini
kwa jambo jingine mmoja aliyepokea moja ya kumi kwa Abrahamu ikaelezwa kama
anayeishi. 9 Na kwa namna ya kuzungumza, Lawi aliyepokea moja ya kumi, pia
alilipa moja ya kumi kwa Abrahamu, 10 kwa sababu Lawi alikuwa katika viuno vya
baba yake Abrahamu wakati Melkizedeki alipokutana na Abrahamu. 11 Sasa kama
ukamilifu uliwezekana kupitia ukuhani wa Lawi, (hivyo chini yake watu hupokea
sheria), kulikuwa na hitaji gani zaidi kwa kuhani mwingine kuinuka baada ya
mfumo wa Melkizedeki, na siyo kuitwa baada ya mpangilio wa Haruni? 12 Kwa hiyo
ukuhani ukibadilika, hapana budi sheria nayo kubadilika. 13 Kwa mmoja ambaye
mambo haya yalisemwa kuhusu kabila jingine, kutoka kwake hakuna aliyehudumu
madhabahuni. 14 Sasa ni wazi kwamba Bwana wetu alitoka katika Yuda, kabila
ambalo Musa hakutaja kuhusu makuhani. 15 Na haya tusemayo ni wazi hasa ikiwa
kuhani mwingine atatokea kwa mfano wa Melkizedeki. 16 Kuhani huyu mpya siyo
mmoja ambaye amekuwa kuhani juu ya msingi wa sheria zinazohusiana na uzao
wa mtu, lakini katika msingi wa nguvu ya maisha yasiyoweza kuharibika. 17 Hivyo
maandiko yanashuhudia kuhusu yeye: "Wewe ni kuhani milele baada ya mfumo
wa Melkizedeki." 18 Kwa kuwa amri iliyotangulia iliwekwa pembeni kwa sababu
ilikuwa dhaifu na haifai. 19 Hivyo sheria haikufanya chochote kikamilifu. Isipokuwa,
kulikuwa na ujasiri mzuri kwa hayo tunamsogelea Mungu. 20 Na Ujasiri huu mzuri
haukutokea pasipo kuzungumzia kiapo, kwa hili makuhani wengine hawakuchukua
kiapo chochote. 21 Lakini Mungu alichukua kiapo wakati aliposema kuhusu Yesu,
"Bwana ameapa na hatabadilisha mawazo yake.' wewe ni kuhani milele." 22 Kwa
hili Yesu pia amekuja kuwa dhamana ya agano bora. 23 Kwa hakika, kifo huzuia
makuhani kuhudumu milele. Hii ni kwa sababu walikuwapo makuhani wengi,
mmoja baada ya mwingine. 24 Lakini kwa sababu Yesu anaishi milele, ukuhani wake
haubadiliki. 25 Kwa hiyo yeye pia anaweza kwa ukamilifu kukamilisha kuwaokoa
wanaomkaribia Mungu kupitia kwake, kwa kuwa yeye anaishi daima kwa kuomba
kwa ajili yao. 26 Kwa hiyo kuhani mkuu wa namna hii anastahili kwetu. Asiye
na dhambi, hatia, msafi, aliyetengwa kutoka kwa wenye dhambi, na amekuwa juu
kuliko mbingu. 27 Yeye hakuwa na uhitaji, mfano wa makuhani wakuu, kutoa
dhabihu kila siku, kwanza kwa dhambi yake mwenyewe, na baadaye kwa dhambi za
watu. Alifanya hivi mara moja kwa wote, alipojitoa yeye mwenyewe. 28 Kwa sheria
huwateua watu dhaifu kuwa makuhani wakuu, lakini neno la kiapo, lililokuja baada
ya sheria, alimteua Mwana, aliyefanywa kuwa mkamilifu milele.

# 8

1 Sasa jambo ambalo tunasema ni hili: tunaye kuhani mkuu aliyekaa chini katika
mkono wa kulia wa kiti cha enzi Mbinguni. 2 Yeye ni mtumishi katika mahali
patakatifu, hema la kweli ambalo Bwana ameliweka, siyo mtu yeyote wa kufa.
3 Kwa maana kila kuhani mkuu huwekwa kutoa zawadi na dhabihu; kwa hiyo
ni muhimu kuwa na kitu cha kutoa. 4 Sasa kama Kristo alikuwa juu ya nchi,
yeye asingekuwa kuhani zaidi ya hapo. Kwa kuwa walikuwa tayari wale waliotoa
vipawa kulingana na sheria. 5 Walihudumu kitu ambacho kilikuwa nakala na kivuli
cha vitu vya mbinguni, sawa kama Musa alipoonywa na Mungu wakati alipotaka
kujenga hema. "Ona," Mungu akasema, "kwamba tengeneza kila kitu kulingana

na muundo ulioonyeshwa juu ya mlima”. 6 Lakini sasa Kristo amepokea huduma
bora zaidi kwa sababu yeye pia ni mpatanishi wa agano zuri, ambalo limekwisha
kuimarishwa kwa ahadi nzuri. 7 Hivyo kama agano la kwanza lisingekuwa na
makosa, ndipo hakungekuwa na haja kutafuta agano la pili. 8 Kwa kuwa wakati
Mungu alipogundua makosa kwa watu alisema, “Tazama, siku zinakuja, 'asema
Bwana, 'wakati nitakapotengeneza agano jipya pamoja na nyumba ya Israeli, na
nyumba ya Yuda. 9 Halitakuwa kama agano nililofanya pamoja na baba zao siku
ambayo niliwachukua kwa mkono kuwaongoza kutoka nchi ya Misri. Kwa kuwa
hawakuendelea katika agano langu, nami sikuwajali tena,' asema Bwana. 10 Kwa
kuwa hili ndilo agano nitafanya kwa nyumba ya Israeli baada ya siku hizo,' asema
Bwana. 'nitaweka sheria zangu mawazoni mwao, na nitaziandika mioyoni mwao.
Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. 11 Hawatafundishana kila mmoja
na jirani yake, na kila mmoja na ndugu, yake, akisema, “Mjue Bwana,” hivyo wote
watanijua mimi, kutoka mdogo hadi mkubwa wao. 12 Hivyo nitaonyesha rehema kwa
matendo yao yasiyo ya haki, na sizitazikumbuka dhambi zao tena.” 13 Kwa kusema
“Mpya,” amelifanya agano la kwanza kuwa kuukuu. Na hilo ambalo amelitangaza
kuwa kuukuu liko tayari kutoweka.

# 9

1 Sasa hata agano la kwanza lilikuwa na sehemu ya ibada hapa duniani na
taratibu za ibada. 2 Kwani katika hema kulikuwa na chumba kimeandaliwa, chumba
cha nje, paliitwa mahali patakatifu. Katika eneo hili palikuwa na kinara cha taa,
meza na mikate ya wonyesho. 3 Na nyuma ya pazia la pili kulikuwa na chumba
kingine, paliitwa mahali patakatifu zaidi. 4 Mlikuwemo madhabahu ya dhahabu kwa
kuvukizia uvumba. Pia mlikuwemo sanduku la agano, ambalo lilikuwa limejengwa
kwa dhahabu tupu. Ndani yake kulikuwa na bakuli la dhahabu lenye manna, fimbo
ya Haruni iliyoota majani, na zile mbao za mawe za agano. 5 Juu ya sanduku la
agano maumbo ya maserafi wa utukufu wafunika mabawa yao mbele ya kiti cha
upatanisho, ambacho kwa sasa hatuwezi kuelezea kwa kina. 6 Baada ya vitu hivi
kuwa vimekwisha andaliwa, Makuhani kawaida huingia chumba cha nje cha hema
kutoa huduma zao. 7 Lakini kuhani mkuu huingia kile chumba cha pili pekee mara
moja kila mwaka, na pasipo kuacha kutoa dhabihu kwa ajili yake binafsi, na kwa
dhambi za watu walizozitenda pasipo kukusudia. 8 Roho Mtakatifu anashuhudia
kwamba, njia ya mahali patakatifu zaidi bado haijafunuliwa kwa vile ile hema
la kwanza bado linasimama. 9 Hili ni kielelezo cha muda huu wa sasa. Vyote
zawadi na dhabihu ambavyo vinatolewa sasa haviwezi kukamilisha dhamiri ya
anayeabudu. 10 Ni vyakula na vinywaji pekee vimeunganishwa katika namna ya
taratibu za ibada ya kujiosha. Vyote hivi vilikuwa taratibu za kimwili vilivyokuwa
vimeandaliwa hadi ije amri mpya itakayowekwa mahali pake. 11 Kristo alikuja kama
kuhani mkuu wa mambo mazuri ambayo yamekuja. kupitia ukuu na ukamilifu
wa hema kuu ambayo haikufanywa na mikono ya watu, ambayo si wa ulimwengu
huu ulioumbwa. 12 Ilikuwa si kwa damu ya mbuzi na ndama, bali kwa damu yake
mwenyewe kwamba Kristo aliingia mahali patakatifu zaidi mara moja kwa kila
mmoja na kutuhakikishia ukombozi wetu wa milele. 13 Kama kwa damu ya mbuzi na
mafahari na kunyunyiziwa kwa majivu ya ndama katika hao wasiosafi walitengwa
kwa Mungu na kufanya miili yao safi, 14 Je si zaidi sana damu ya Kristo ambaye
kupitia Roho wa milele alijitoa mwenyewe bila mawaa kwa Mungu, kuosha dhamiri
zetu kutoka matendo mafu kumtumikia Mungu aliye hai? 15 Kwa sababu hiyo, Kristo
ni mjumbe wa agano jipya. Hii ndiyo sababu mauti imewaacha huru wote walio
wa agano la kwanza kutoka katika hatia ya dhambi zao, ili kwamba wote walioitwa

na Mungu waweze kupokea ahadi ya urithi wao wa milele. 16 Kama kuna agano
linadumu, ni lazima kuthibitishwa kwa kifo cha mtu yule aliyelifanya. 17 Kwani agano
linakuwa na nguvu mahali kunatokea mauti, kwa sababu hakuna nguvu wakati
mwenye kulifanya akiwa anaishi. 18 Hivyo hata si lile agano la kwanza lilikuwa
limewekwa pasipo damu. 19 Wakati Musa alipokuwa ametoa kila agizo la sheria
kwa watu wote, alichukua damu ya ng'ombe na mbuzi, pamoja na maji, kitambaa
chekundu, na hisopo, na kuwanyunyizia gombo lenyewe na watu wote. 20 Kisha
alisema, “Hii ni damu ya agano ambayo Mungu amewapa amri kwenu”. 21 Katika hali
ileile, aliinyunyiza damu juu ya hema na vyombo vyote vilivyotumiwa kwa huduma
ya ukuhani. 22 Na kulingana na sheria, karibu kila kitu kinatakaswa kwa damu.
Pasipo kumwaga damu hakuna msamaha. 23 Kwa hiyo ilikuwa lazima kwamba
nakala za vitu vya mbinguni sharti visafishwe kwa hii dhabihu ya wanyama. Hata
hivyo, vitu vya mbinguni vyenyewe vilipaswa kusafishwa kwa dhabihu iliyo bora
zaidi. 24 Kwani Kristo hakuingia mahali patakatifu sana palipofanywa na mikono,
ambayo ni nakala ya kitu halisi. Badala yake aliingia mbingu yenyewe, mahali
ambapo sasa yuko mbele za uso wa Mungu kwa ajili yetu. 25 Hakuingia kule kwa
ajili ya kujitoa sadaka kwa ajili yake mara kwa mara, kama afanyavyo kuhani mkuu,
ambaye huingia mahali patakatifu zaidi mwaka baada ya mwaka pamoja na damu
ya mwingine, 26 kama hiyo ilikuwa kweli, basi ingekuwa lazima kwake kuteswa mara
nyingi zaidi tangu mwanzo wa ulimwengu. Lakini sasa ni mara moja hadi mwisho wa
miaka aliyojifunua kuiondoa dhambi kwa dhabihu yake mwenyewe. 27 Kama ilivyo
kwa kila mtu kufa mara moja, na baada ya hiyo huja hukumu, 28 ndivyo hivyo Kristo
naye ambaye alitolewa mara moja kuziondoa dhambi za wengi, atatokea mara ya pili,
si kwa kusudi la kushughulikia dhambi, bali kwa ukombozi kwa wale wamgojeao kwa
saburi.

# 10

1 Kwa vile sheria ni kivuli cha mambo mema yajayo, si yale yaliyo halisi.
Sheria kamwe haiwezi kuwakamilisha wale ambao wanaomkaribia Mungu kwa
njia ya dhabihu zilezile ambazo makuhani waliendelea kutoa mwaka baada ya
mwaka. 2 Au vinginevyo dhabihu hizo zisingeweza kukoma kutolewa? Kwa
kigezo hicho waabuduo, wakiwa wamesafishwa mara moja, wasingelikuwa na
utambuzi zaidi wa dhambi. 3 Bali katika dhabihu hizo kuna ukumbusho wa dhambi
zilizotendwa mwaka baada ya mwaka. 4 Kwa kuwa haiwezekani kwa damu ya
mafahari na mbuzi kuziondoa dhambi. 5 Wakati Kristo alipokuja duniani, alisema,
“Hamkutamani matoleo au dhabihu, badala yake, mliandaa mwili kwa ajili yangu.
6 Hamkuwa na thamani katika matoleo yote ya kuteketezwa au dhabihu kwa ajili
ya dhambi. 7 Kisha nilisema, “Ona, hapa ninayafanya mapenzi yako, Mungu, kama
ilivyoandikwa kunihusu mimi katika gombo”. 8 Alisema kama ilivyo semwa hapo juu:
“Hamkutamani dhabihu, matoleo, au sadaka ya kuteketezwa kwa ajili ya dhambi,
wala hukuona furaha ndani yake” dhabihu ambazo zinatolewa kulingana na sheria.
9 Kisha alisema, “Ona, niko hapa kufanya mapenzi yako”. Ameweka pembeni taratibu
zilizo za awali ili kuimarisha zile za pili. 10 Katika taratibu za pili, tumekwisha
tengwa kwa Mungu kwa mapenzi yake kupitia kujitoa kwa mwili wa Yesu Kristo mara
moja kwa nyakati zote. 11 Ni kweli, kila kuhani husimama kwa huduma siku kwa
siku, akitoa dhabihu ile ile, ambayo, kwa vyovyote, kamwe isingeweza kuziondoa
dhambi. 12 Lakini baada ya Kristo kutoa dhabihu mara moja kwa dhambi milele
yote, aliketi mkono wa kuume wa Mungu, 13 akisubiri mpaka maadui zake watiwe
chini na kufanywa kiti kwa ajili ya miguu yake. 14 Kwa kuwa kwa njia ya toleo moja
amewakamilisha milele wale ambao wametengwa kwa Mungu. 15 Na Roho Mtakatifu

pia ashuhudia kwetu. Kwa kuwa kwanza alisema, 16 “Hili ni agano nitakalofanya
pamoja nao baada ya siku hizo; asema Bwana: nitaweka sheria zangu ndani ya
mioyo yao, na nitaziandika katika akili zao”. 17 Kisha alisema, “Hawatazikumbuka
tena dhambi na matendo yao mafu”. 18 Sasa mahali palipo na msamaha kwa hawa,
hakuna tena dhabihu yoyote kwa ajili ya dhambi. 19 Kwa hiyo, ndugu, tunao ujasiri
wa kuingia mahali patakatifu zaidi kwa damu ya Yesu. 20 Hiyo ni njia ambayo
ameifungua kwa ajili yetu kwa njia ya mwili wake, mpya na hai inayopitia kwenye
pazia. 21 Na kwa sababu tunaye kuhani mkuu juu ya nyumba ya Mungu, 22 na
tumkaribie na moyo wa kweli katika utimilifu wa uhakika wa imani tukiwa na mioyo
iliyonyunyiziwa safi kutoka uovu wa dhamiri na kuwa na miili yetu iliyooshwa kwa
maji safi. 23 Basi na tushikilie kwa uthabiti katika ungamo la ujasiri wa tumaini
letu, bila ya kugeuka, kwa sababu Mungu aliyeahidi ni mwaminifu. 24 Na tuzidi
kutafakari namna ya kumtia moyo kila mmoja kupenda na matendo mema. 25 Na
tusiache kukusanyika pamoja, kama wafanyavyo wengine. Badala yake, kutiana
moyo kila mmoja zaidi na zaidi, kama muonavyo siku inakaribia. 26 Kama tukifanya
makusudi kuendelea kutenda dhambi baada ya kuwa tumepokea elimu ya ukweli,
Dhabihu nyingine ya dhambi haisalii tena. 27 Badala yake, kuna tarajio pekee la
hukumu ya kutisha, na ukali wa moto ambao utawateketeza maadui wa Mungu.
28 Yeyote ambaye ameikataa sheria ya Musa hufa bila rehema mbele ya ushuhuda wa
mashahidi wawili au watatu. 29 kiwango gani zaidi cha adhabu unafikiri kinamstahiri
kilammoja ambaye amemdharau mwana wa Mungu, yeyote aliyeitendea damu
ya agano kama kitu kisicho kitakatifu, damu ambayo kwayo aliiweka wakfu kwa
Mungu - yeyote ambaye amemtukana Roho wa neema? 30 Kwakuwa tunajua mmoja
ambaye aliyesema, “Kisasi ni changu, nitalipa”. Na tena, “Bwana atawahukumu
watu wake”. 31 Ni jambo la kuogofya mtu kuangukia katika mikono ya Mungu
aliye hai! 32 Lakini kumbuka siku zilizopita, baada ya kutiwa kwenu nuru, ni
jinsi gani mliweza kuvumilia maumivu makali. 33 Mlikuwa mmewekwa wazi katika
dhihaka ya matukano na mateso, na mlikuwa washiriki pamoja na wale waliopitia
mateso kama hayo. 34 Kwa kuwa mlikuwa na moyo wa huruma kwa hao waliokuwa
wafungwa, na mlipokea kwa furaha adhabu ya urithi wenu, mkijua kwamba ninyi
wenyewe mlikuwa na urithi bora na wa kudumu milele. 35 Kwa hiyo msiutupe ujasiri
wenu, ulio na zawadi kuu. 36 Kwa kuwa mnahitaji uvumilivu, ili kwamba mpate
kupokea ambacho Mungu amekiahidi, baada ya kuwa mmekwisha yatenda mapenzi
yake. 37 Kwa kuwa baada ya kitambo kidogo, mmoja anayekuja, atakuja hakika
na hatakawia. 38 Mwenye haki wangu ataishi kwa imani. Kama atarudi nyuma,
sitapendezwa naye.” 39 Lakini sisi si kama wale warudio nyuma kwa kuangamia.
Badala yake, sisi ni baadhi ya wale tulio na imani ya kuzilinda roho zetu.

## 11

1 Sasa imani ni hakika aliyo nayo mtu wakati atarajiapo kitu fulani kwa ujasiri.
Ni hakika ya kitu ambacho bado hakijaonekana. 2 Kwa sababu hii mababu
zetu walithibitika kwa imani yao. 3 Kwa imani tunafahamu kwamba ulimwengu
uliumbwa kwa amri ya Mungu, ili kwamba kile kinachoonekana hakikutengenezwa
kutokana na vitu ambavyo vilikuwa vinaonekana. 4 Ilikuwa kwa sababu ya imani
kwamba Habili alimtolea Mungu sadaka ya kufaa kuliko alivyofanya Kaini. Ilikuwa ni
kwa sababu hii kwamba alisifiwa kuwa mwenye haki. Mungu alimsifu kwa sababu ya
zawadi alizoleta. Kwa sababu hiyo, Habili bado ananena, ingawa amekufa. 5 Ilikuwa
kwa imani kwamba Enoko alichukuliwa juu na hakuona mauti. “Hakuonekana,
kwa sababu Mungu alimchukua” kwa vile ilinenwa juu yake kuwa alimpendeza
Mungu kabla ya kuchukuliwa juu. 6 Pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu,

kwa kuwa ajaye kwa Mungu lazima aamini kwamba Mungu anaishi na kwamba
huwapatia zawadi wale wamtafutao. 7 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Nuhu, akiwa
ameonywa na Mungu kuhusiana na mambo ambayo hayakuwa yameonekana, kwa
heshima ya ki Mungu alitengeneza safina kwa ajili ya kuiokoa familia yake. Kwa
kufanya hivi, aliuhukumu ulimwengu na akawa mrithi wa haki ambayo huja kupitia
imani. 8 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Ibrahimu, alipoitwa alitii na kwenda mahali
ambapo alipaswa kupokea kama urithi. Alitoka bila kujua mahali gani alikuwa
anakwenda. 9 Ilikuwa ni kwa imani kwamba aliishi katika nchi ya ahadi kama
mgeni. Aliishi katika mahema pamoja na Isaka na Yakobo, warithi wenzake wa
ahadi ile ile. 10 Hii ni kwa sababu alitarajia kuupata mji ambao mwenye kuubuni
na mjenzi wake angelikuwa ni Mungu. 11 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Ibrahimu,
na Sara mwenyewe, walipokea nguvu ya kutunga mimba ingawa walikuwa wazee
sana, kwa kuwa walimuona Mungu kuwa mwaminifu, ambaye aliwaahidia mtoto wa
kiume. 12 Kwa hiyo pia kutoka kwa mtu huyu mmoja ambaye alikuwa amekaribia
kufa wakazaliwa watoto wasiohesabika. Walikuwa wengi kama nyota za angani na
wengi kama mbegu za mchanga katika ufukwe wa bahari. 13 Hawa wote walikufa
katika imani pasipo kupokea ahadi. Isipokuwa, wakiwa wameziona na kuzikaribisha
kwa mbali, walikiri kwamba walikuwa wageni na wapitaji juu ya nchi. 14 Kwa
wale wasemao mambo kama haya wanaweka bayana kuwa wanatafuta nchi yao
wenyewe. 15 Kwa kweli, kama wangekuwa wakiifikiria nchi ambayo kwayo walitoka,
wangelikuwa na nafasi ya kurejea. 16 Lakini kama ilivyo, wanatamani nchi iliyo
bora, ambayo, ni ya kimbingu. Kwa hiyo Mungu haoni aibu kuitwa Mungu wao, kwa
kuwa ametayarisha mji kwa ajili yao. 17 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Ibrahimu
baada ya kujaribiwa, alimtoa Isaka. Ndiyo, yeye ambaye alipokea kwa furaha
ahadi, alimtoa mwanawe wa pekee, 18 ambaye juu yake ilinenwa, “Kutoka kwa
Isaka uzao wako utaitwa.” 19 IbrahImU alijua kwamba Mungu alikuwa na uwezo
wa kumfufua Isaka kutoka katika wafu, na kwa kuzungumza kwa lugha ya maumbo,
alimpokea. 20 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Isaka alimbariki Yakobo na Esau kuhusu
mambo yajayo. 21 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Yakobo alipokuwa katika hali ya
kufa, alimbariki kila mmoja wa watoto wa Yusufu. Yakobo akaabudu, akiegemea
juu ya fimbo yake. 22 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Yusufu wakati wake wa
mwisho ulipokaribia, alinena juu ya kutoka kwa wana wa Israel Misri na akawaagiza
kuchukua pamoja nao mifupa yake. 23 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Musa,
alipozaliwa, alifichwa kwa miezi mitatu na wazazi wake kwa sababu walimuona
kuwa ni mtoto mchanga aliyekuwa mzuri, na hawakutishwa na amri ya mfalme.
24 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Musa, alipokuwa mtu mzima, alikataa kuitwa
mtoto wa binti Farao. 25 Badala yake, alichagua kushiriki mateso pamoja na watu
wa Mungu badala ya kufurahia anasa za dhambi kwa kitambo. 26 Alifikiri aibu
ya kumfuata Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri kwa kuwa alikaza
macho yake katika zawadi ya wakati wake ujao. 27 Ilikuwa ni kwa imani kwamba
Musa alitoka Misri. Hakuhofia hasira ya Mfalme, kwa kuwa alivumilia kwa kutazama
kwa asiyeonekana. 28 Ilikuwa ni kwa imani kwamba aliishika pasaka na kunyunyiza
damu, ili kwamba mharibu wa mzaliwa wa kwanza asiweze kuwagusa wazaliwa wa
kwanza wa kiume wa waisrael. 29 Ilikuwa ni kwa imani kwamba walipita katika
bahari ya shamu kama katika nchi kavu. Wakati wamisri walipojaribu kupita,
walimezwa. 30 Ilikuwa ni kwa imani kwamba ukuta wa Yeriko ulianguka chini, baada
ya kuuzunguka kwa siku saba. 31 Ilikuwa ni kwa imani kwamba Rahabu yule kahaba
hakuangamia pamoja na wale ambao hawakuwa watiifu, kwa sababu alikuwa
amewapokea wapelelezi na kuwahifadhi salama. 32 Na niseme nini zaidi? Maana
muda hautoshi kusimulia ya Gideoni, Barak, Samsoni, Yeftha, Daudi, Samwel na za

manabii, [33] ambao kupitia imani walizishinda falme, walitenda haki, na wakapokea
ahadi. Walizuia vinywa vya simba, [34] walizima nguvu za moto, walikwepa ncha
ya upanga, waliponywa kutoka katika magonjwa, walikuwa mashujaa vitani, na
walisababisha majeshi wageni kukimbia. [35] Wanawake walipokea wafu wao kwa
njia ya ufufuo. Wengine waliteswa, bila kukubali kuachwa huru ili kwamba waweze
kupata uzoefu wa ufufuo ulio bora zaidi. [36] Wengine waliteswa kwa dhihaka na
kwa vichapo, naam, hata kwa vifungo na kwa kutiwa gerezani. [37] Walipondwa
mawe. Walikatwa vipande kwa misumeno. Waliuawa kwa upanga. Walikwenda
kwa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi walikuwa wahitaji, wakiendelea katika
maumivu na wakitendewa mabaya [38] (ambayo ulimwengu haukustahili kuwa nao),
wakitangatanga nyikani, milimani, katika mapango na katika mashimo ya ardhini.
[39] Ingawa watu wote hawa walikubaliwa na Mungu kwa sababu ya imani yao,
hawakupokea alichoahidi. [40] Mungu alitangulia kutupatia kitu kilichobora, ili
kwamba bila sisi wasingeweza kukamilishwa.

# 12

[1] Kwahiyo, kwa kuwa tumezungukwa na wingu kubwa la mashaidi, na tutupe
kila kitu kinacho tulemea pamoja na dhambi ambayo inatuzingira kwa urahisi.
Tupige mbio kwa saburi katika mashindano yaliyowekwa mbele yetu. [2] Tuyaelekeze
macho yetu kwa Yesu, aliye mwanzilishi na mwenye kutimiliza imani yetu, ambaye
kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake alistahmili msalaba, akiidharau aibu
yake, na akakaa chini mkono wa kulia wa kiti cha enzi cha Mungu. [3] Maana
mtafakarini yeye aliye stahimili maneno ya chuki kutoka kwa wenye dhambi, dhidi
yake mwenyewe ili kwamba msije mkachoka au kuzimia mioyo yenu. [4] Hamjataabika
au kuteseka mkishindana na dhambi kiasi cha kuishiwa damu. [5] Tena mmesahau
kule kutiwa moyo ambako kunawaelekeza kama watoto wa kiume: "Mwanangu,
usiyachukuwe kwa wepesi marudia ya Bwana, wala usikate tamaa unapo rekebishwa
na yeye." [6] Kwa kuwa Bwana humrudi yeyote ambaye anampenda, na humwadhibu
kila mwana ambaye humpokea. [7] Stahimili majaribu kama kurudiwa. Mungu
hushughulika nanyi kama anavyoshughulika na watoto, maana ni mtoto yupi ambaye
baba yake hawezi kumrudi? [8] Lakini kama hakuna kurudiwa, ambako sisi sote
tunashiriki, basi ninyi ni haramu na si watoto wake. [9] Zaidi ya yote, tulikuwa na
baba zetu kidunia wa kuturudi, na tuliwaheshimu. Je haitupasi hata zaidi kumtii
Baba wa kiroho na kuishi? [10] Kwa hakika baba zetu walituadhibu kwa miaka
michache kama ilivyoonekana sawa kwao, lakini Mungu hutuadhibu kwa faida
yetu ili tushiriki utakatifu wake. [11] Hakuna adhabu inayofurahisha kwa wakati
huo. Huwa na maumivu. Hata hivyo, baadaye huzaa tunda la amani ya utauwa
kwa wale waliofundishwa nayo. [12] Kwa hiyo inueni mikono yenu iliyolegea na
kufanya magoti yenu yaliyo dhaifu kuwa yenye nguvu tena; [13] nyosheni mapito ya
nyayo zenu, ili kwamba yeyote aliye mlemavu hataongozwa upotevuni lakini apate
kuponywa. [14] Tafuteni amani na watu wote, na pia utakatifu ambao bila huo hakuna
atakayemwona Bwana. [15] Muwe waangalifu ili kwamba asiwepo atakayetengwa
mbali na neema ya Mungu, na kwamba lisije shina la uchungu litakalochipuka na
kusababisha shida na kukengeusha wengi. [16] Angalieni kuwa hakuna zinaa au mtu
asiye mtauwa kama vile Esau, ambaye kwa sababu ya mlo mmoja aliuza haki yake
ya kuzaliwa. [17] Kwa kuwa mnajua kwamba baadaye, alipotamani kurithi baraka,
alikataliwa, kwa sababu hakupata fursa ya kutubu pamoja na baba yake, hata ingawa
alitafuta sana kwa machozi. [18] Kwa kuwa hamkuja katika mlima ambao unaweza
kuguswa, Mlima unaowaka moto, giza, kukatisha tamaa na dhoruba. [19] Hamkuja
kwa sauti za tarumbeta, au kwa maneno yatokanayo na sauti ambayo ilisababisha

kila wasikiao wasiombe neno lolote kusemwa kwao. [20] Kwa kuwa hawakuweza
kuvumilia kile kilichoamuliwa: “Ikiwa hata mnyama agusaye mlima, lazima apigwe
kwa mawe.” [21] Ya kutisha zaidi aliyoyaona Musa alisema, “Nimeogopa sana kiasi
cha kutetemeka”. [22] Badala yake, mmekuja mlima Sayuni na katika mji wa Mungu
aliye hai, Yerualem ya mbinguni, na kwa malaika elfu kumi wanaosherehekea.
[23] Mmekuja katika kusanyiko la wazaliwa wa kwanza wote waliosajiliwa mbinguni,
kwa Mungu hakimu wa wote, na kwa roho za watakatifu ambao wamekamilishwa.
[24] Mmekuja kwa Yesu mpatanishi wa agano jipya, na kwa damu iliyonyunyizwa
ambayo hunena mema zaidi kuliko damu ya Habili. [25] Angalia kuwa usije ukamkataa
mmoja ambaye anenaye. Kwa kuwa kama hawakuepuka walipomkataa mmoja aliye
waonya duniani, kwa hakika hatutaepuka ikiwa tutageuka mbali kutoka kwa yule
atuonyaye kutoka mbinguni. [26] Kwa wakati huo sauti yake ilitikisa dunia. Lakini
sasa ameahidi na kunena, “Bado mara nyingine tena sitatikisa dunia pekee, bali
mbingu pia.” [27] Maneno haya, “Mara moja tena,” inaonesha kutoweshwa kwa vitu
vile vitetemeshwavyo, hivi ni, vitu vile ambavyo vimeumbwa, ili kwamba vile vitu
visivyotetemeshwa vibakie. [28] Kwa hiyo, tupokee ufalme ambao hautetemeshwi,
tufurahi katika hali ya kumwabudu Mungu kwa kukubali pamoja na kunyenyekea
katika kicho, [29] kwa maana Mungu wetu ni moto ulao.

# 13

[1] Basi upendo wa ndugu na uendelee. [2] Msisahau kuwakaribisha wageni, maana
kwa kufanya hivi, baadhi wamewakaribisha malaika pasipo kujua. [3] Kumbuka wote
waliomo gerezani, kana kwamba mulikuwa nao kule pamoja nao, na kama miili
yenu ilitendewa kama wao. [4] Basi ndoa na iheshimiwe na wote na basi kitanda cha
ndoa kifanywe kuwa safi, kwa maana Mungu atawahukumu waasherati na wazinzi.
[5] Basi njia zenu za maisha ziwe huru katika upendo wa pesa. Muwe wanoridhika na
vitu mulivyonavyo, kwani Mungu mwenyewe alisema, “Sitawaacha ninyi kamwe,
wala kuwatelekeza ninyi.” [6] Basi tulidhikeni ili tusema kwa ujasiri, “Bawa ni
msaidizi wangu; Sitaogopa. Mwanadamu aweza kunifanya nini?” [7] Wafikirieni wale
walio waongoza, wale waliongea neno la Mungu kwenu, na kumbukeni matokeo ya
mienendo yao; igeni imani zao. [8] Yesu Kristo ni yeye jana, leo, na ata milele. [9] Usije
ukaongozwa na mafundisho mbalimbali ya kigeni kwani ni vizuri kwamba moyo
ujengwe kwa neema, na siyo kwa sheria kuhusu chakula hayo hayatawasaidia wale
wanaoishi kwa hayo. [10] Tunayo madhabau ambayo wale wanaotumika ndani ya
hekalu hawana haki ya kula. [11] Kwa kuwa damu za wanyama, zilizotolewa dhabihu
kwa ajili ya dhambi, ililetwa na kuhani mkuu ndani ya sehemu takatifu, lakini miili
yao ilichomwa nje ya kambi. [12] Kwa hiyo Yesu naye aliteseka nje ya lango la mji,
hili kwamba kuweka wakfu watu kwa Mungu kupitia damu yake. [13] Na kwa hiyo
twendeni kwake nje ya kambi, tukizibeba fadheha zake. [14] Kwani hatuna makao ya
kudumu katika mji huu. Badala yake tutafute mji ambao unakuja. [15] Kupitia Yesu
mnapaswa mara kwa mara kujitoa sadaka ya kumtukuza Mungu, kumsifu kwamba
tunda la midomo yetu likili jina lake. [16] Na usisahau kufanya mazuri na kusadiana
ninyi kwa ninyi, kwa kuwa ni kwa sadaka kama hiyo ndiyo Mungu hupendezwa sana.
[17] Tiini na kujishusha kwa viongozi wenu, kwani wanaendelea kuwalinda kwa ajili ya
nafsi zenu, kama wale watakaotoa hesabu. Tiini ili kwamba viongozi wenu waweze
kuwatunza kwa furaha, na sio kwa huzuni, ambayo haitawasaidia. [18] Tuombeni,
kwani tuna uhakikwa kwamba tuna dhamira njema, tunatamani kuishi maisha ya
heshima katika mambo yote. [19] Na nyote ninawatia moyo zaidi mfanye hivi, ili
kwamba niweze kurudi kwenu hivi karibuni. [20] Sasa Mungu wa amani, ambaye
aliwaleta tena kutoka kwa wafu mchungaji mkuu wa kondoo, Bwana wetu Yesu, kwa

damu ya agano la milele, 21 Atawapa uwezo kwa kila jambo zuri kufanya mapenzi
yake, akifanya kazi ndani yetu iliyo njema ya kupendeza machoni pake, kupitia
Yesu Kristo, kwake uwe utukufu milele na milele. Amina. 22 Sasa ninakutia moyo,
ndugu, kuchukualiana na neno la kutia moyo ambalo kwa ufupi nililiandika kwenu.
23 Fahamu kwamba ndugu yetu Timotheo ameshaachiwa huru, ambaye pamoja naye
nitawaona kama atakuja hivi karibuni. 24 Salimia viongozi wako wote na waumini
wote. Wale wanaotoka Italia wanakusalimia. 25 Na neema iwe nanyi nyote.

# Waraka wa Yakobo

1 Yakobo, mtumwa wa Mungu na wa Bwana Yesu Kristo, kwa makabila kumi
na mbili yaliyotawanyika, salaam. 2 Hesabuni kuwa ni furaha zaidi, ndugu zangu,
mnapopita katika matatizo mbali mbali, 3 mkijua kuwa kujaribiwa kwa imani yenu
huwapa uvumilivu. 4 Acheni uvumilivu uikamilishe kazi yake, kwamba muweze
kukomaa kikamilifu, bila kupungukiwa katika lolote. 5 Lakini kama mtu kati yenu
anahitaji hekima, aiombe kutoka kwa Mungu, ambaye hutoa kwa ukarimu na pasipo
kukemea kwa wote wamwombao, na atawapa hekima. 6 Lakini omba kwa imani, bila
shaka, kwa kuwa mwenye kutia shaka ni kama mawimbi katika bahari, huchukuliwa
na upepo na kutupwa huku na huko. 7 Kwa hakika mtu huyu asifikirie kwamba
atapokelewa ombi lake kutoka kwa Bwana; 8 mtu huyu ana nia mbili, si imara katika
njia zake zote. 9 Ndugu maskini anapaswa kujivuna katika kusimama kwake juu,
10 wakati huo huo ndugu tajiri katika unyenyekevu wake, kwa sababu atatoweka
kama ua la kondeni katika shamba analopita. 11 Jua huchomoza na joto la kuunguza
kukausha mimea, na maua huanguka na uzuri wake hufa. Vivyo hivyo watu matajiri
watachakaa katikati ya kazi zao. 12 Amebarikiwa mtu yule anayevumilia majaribu,
kwa kuwa baada ya kushinda jaribu hilo, atapokea taji ya uzima, ambayo imeahidiwa
kwa wale wampendao Mungu. 13 Mtu yeyote hapaswi kusema anapojaribiwa,
"Jaribu hili linatoka kwa Mungu," kwa sababu Mungu hajaribiwi na uovu, na
Mungu mwenyewe hamjaribu yeyote. 14 Kila mtu hujaribiwa na tamaa zake mbaya
zinazomshawishi na kumvuta mbali. 15 Ndipo baada ya tamaa ya dhambi kubeba
mimba, dhambi huzaliwa, na baada ya dhambi kukomaa sawasawa, huishia katika
mauti. 16 Ndugu zangu wapendwa, msidanganyike. 17 Kila zawadi iliyo nzuri na kila
zawadi iliyokamilika hutoka juu, hushuka chini kutoka kwa Baba wa nuru. Kamwe
habadiliki kama kivuli kibadilikavyo. 18 Mungu alichagua kutupa sisi uzima kwa
Neno la kweli, ili kwamba tuweze kuwa kama uzao wa kwanza miongoni mwa
viumbe vyake. 19 Mnajua hili, ndugu zangu wapendwa. Kila mmoja anapaswa
kuwa mwepesi wa kusikia, siyo mwepesi wa kuongea wala kukasirika, 20 kwa kuwa
hasira ya mwanadamu haiwezi kutenda haki ya Mungu. 21 Kwa hiyo wekeni mbali
uchafu wa dhambi na ubaya wote ulio mahali popote, na kwa unyenyekevu lipokeeni
neno lililopandwa ndani yenu, ambalo lina uwezo wa kuokoa roho zenu. 22 Litiini
neno, msilisikie tu, mkijidanganya nafsi zenu wenyewe. 23 Kwa kuwa kama yeyote
alisikiaye neno bila kulitendea kazi ni sawa na mtu ajiangaliaye uso wake halisi katika
kioo. 24 Hujitathimini uso wake, na huenda zake na baada ya muda mfupi husahau
anavyofanana. 25 Bali mtu yule anayeiangalia kwa uangalifu sheria kamili, sheria
ya uhuru, na kuendelea kuitii, si kwa sababu yeye ni msikilizaji anayesahau, huyu
mtu atabarikiwa anapoitenda. 26 Ikiwa mtu yeyote atafikiri mwenyewe kuwa ni mtu
wa dini, lakini hawezi kuutawala ulimi wake, huudanganya moyo wake na dini yake
ni bure. 27 Dini iliyo safi na isiyoharibiwa mbele za Mungu wetu na Baba ni hii:
kuwasaidia yatima na wajane katika mateso yao, na kujilinda wenyewe na ufisadi
wa dunia.

## 2

1 Ndugu zangu msiifuate imani ya Bwana Yesu Kristo, Bwana wa utukufu, kwa
kupendelea watu fulani. 2 Kama mtu fulani akiingia kwenye mikutano yenu amevaa
pete za dhahabu na mavazi mazuri, pia akaingia masikini mwenye mavazi machafu,
3 na mkaonyesha kumjali zaidi yule mwenye mavazi mazuri na kusema, "Tafadhari

wewe keti hapa mahali pazuri" lakini mkamwambia yule masikini, "Wewe simama
pale," au "Kaa chini ya miguu yangu." 4 Je, hamuhukumiani ninyi wenyewe, na
kuwa waamuzi wenye mawazo mabaya? 5 Sikilizeni, ndugu zangu wapendwa, je,
Mungu hakuwachagua masikini wa dunia kuwa matajiri katika imani na kurithi
ufalme aliowaahidia wampendao? 6 Lakini mmewadharau masikini! Je, sio matajiri
wanaowatesa ninyi, na sio wao wanaowaburuta mahakamani? 7 Je, si matajiri
wanaolitukana jina lile zuri ambalo kwalo mnaitiwa? 8 Hata hivyo, kama mwaitimiza
ile sheria ya kifalme kama ilivyoandikwa katika maandiko, "Utampenda jirani yako
kama wewe mwenyewe," mwafanya vyema. 9 Lakini kama mkipendelea baadhi ya
watu, mnatenda dhambi, mwahukumiwa na sheria kuwa ni wavunja sheria. 10 Kwa
kuwa yeyote atiiye sheria yote, na bado akajikwaa katika nukta moja tu, amekuwa
na hatia ya kuvunja sheria yote! 11 Kwa kuwa Mungu aliyesema, "Usizini," ndiye
pia aliyesema, "Usiue." Kama hauzini, lakini una uwa, umekwishavunja sheria ya
Mungu. 12 Kwa hiyo zungumzeni na kutii kama wale ambao mko karibu kuhukumiwa
na sheria ya uhuru. 13 Kwa kuwa hukumu huja pasipo huruma kwa wale wasio na
huruma. Huruma hujitukuza juu ya hukumu. 14 Kuna uzuri gani, ndugu zangu, kama
mtu anasema ninayo imani, lakini hana matendo? Je, imani hiyo yaweza kumwokoa?
15 Kama ndugu wa kiume au wa kike ni muhitaji wa mavazi au chakula cha kila siku,
16 na mmoja wenu akawaambia, "Nendeni kwa amani, mkaote moto na mle vizuri,"
lakini hamuwapi mahitaji muhimu ya mwili, hiyo yafaaa nini? 17 Hali kadhalika,
imani pekee, kama haina matendo, imekufa. 18 Bado mtu fulani anaweza kusema, "
Una imani, na mimi ninayo matendo." Nionyeshe imani yako pasipo matendo, nami
nitakuonyesha imani yangu kwa matendo yangu. 19 Waamini kuwa kuna Mungu
mmoja; uko sahihi. Lakini mapepo nayo yanaamini hivyo na kutetemeka. 20 Je,
unataka kujua, ewe mtu mpumbavu, namna ambavyo imani hiyo pasipo matendo
isivyofaa? 21 Je, si baba yetu Abrahamu alihesabiwa haki kwa matendo alipomtoa
mwanawe Isaka juu ya madhabahu? 22 Mnaona kuwa imani yake ilifanya kazi na
matendo yake, na kwa matendo yake, imani yake ilifikia kusudio lake. 23 Maandiko
yalitimizwa yasemayo, "Abrahamu alimwamini Mungu, na akahesabiwa kuwa ni
mwenye haki." Hivyo Abrahamu aliitwa rafiki wa Mungu. 24 Mwaona kuwa kwa
matendo mtu huhesabiwa haki, na si kwa imani tu. 25 Hali kadhalika, je, hakuwa
Rahabu yule kahaba alihesabiwa haki kwa matendo, alipowakaribisha wajumbe na
kuwapeleka kwa barabara nyingine? 26 Kwa kuwa kama vile mwili usipokuwa na
roho umekufa, vivyo hivyo imani pasipo matendo imekufa.

# 3

1 Ndugu zangu, siyo wengi wenu mnapaswa kuwa walimu, mkijua kwamba
tutapokea hukumu kubwa zaidi. 2 Kwa kuwa wote tunakosea katika njia nyingi.
Kama yeyote huwa hajikwai katika maneno yake, huyo ni mtu mkamilifu, aweza
kudhibiti mwili wake wote pia. 3 Sasa kama tunaweka lijamu za farasi katika vinywa
vyao wanatutii, na tunaweza kuigeuza miili yao yote. 4 Tambua pia kwamba meli,
ingawa ni kubwa na husukumwa na upepo mkali, zinaongozwa kwa usukani mdogo
sana kwenda popote anakotaka nahodha. 5 Vivyo hivyo, ulimi ni kiungo kidogo cha
mwili, lakini hujisifia makuu sana. Angalia msitu mkubwa unavyoweza kuwashwa
kwa cheche ndogo ya moto! 6 Ulimi pia ni moto, ni ulimwengu wa uovu, umewekwa
miongoni mwa viungo vya mwili wetu, ambao hunajisi mwili wote na huiweka juu
ya moto njia ya maisha, na wenyewe kuchomwa moto wa kuzimu. 7 Kila aina ya
mnyama wa polini, ndege, kitambaacho na kiumbe cha baharini kinadhibitiwa na
wanadamu. 8 lakini hakuna mwanadamu hata mmoja ambaye anaweza kudhibiti
ulimi; ni uovu usiotulia, umejaa sumu ya kufisha. 9 Kwa ulimi twamtukuza Bwana na

Baba yetu, na kwa huo twawalaani watu ambao wameumbwa kwa mfano wa Mungu.
10 Katika kinywa hichohicho husema maneno ya baraka na laana. Ndugu zangu
mambo haya hayapaswi kuwa. 11 Je, kisima kimoja huweza kutoa maji matamu na
machungu? 12 Ndugu zangu, Je, mti wa mtini unaweza kuzaa matunda ya mzeituni,
au mzabibu unazaa matunda ya mtini? Wala chemchemi ya maji chumvi haitoi maji
yasio na chumvi. 13 Ni nani miongoni mwenu aliye na hekima na ufahamu? Hebu
mtu huyo na aoneshe maisha mema katika kazi zake kwa unyenyekevu utokanao
na hekima. 14 Lakini kama mnao wivu mkali na nia ya ubinafsi mioyoni mwenu,
msijivune na kusema uongo mkiupinga ukweli. 15 Hii siyo hekima ile ishukayo kutoka
juu, lakini badala yake ni ya kidunia, si ya kiroho, na ni ya kipepo. 16 Kwa kuwa palipo
na wivu na ubinafsi upo, kuna vurugu na kila matendo maovu 17 Lakini hekima
itokayo juu, kwanza ni safi, kisha kupenda amani, upole na ukarimu, yenye kujaa
rehema na matunda mema, bila kupendelea watu fulani, na kweli. 18 Na tunda la
haki hupandwa katika amani kwa wale ambao wanatenda mambo ya amani.

# 4

1 Ugonvi na migogoro miongoni mwenu vyatoka wapi? Haviinuki kutoka katika
tamaa zenu mbaya zinazoleta vita ndani ya washirika wenu? 2 Mnatamani
kile msichokuwa nacho. Mnauwa na mnafukuzia kile msichoweza kuwa nacho.
Mnapigana na kugombana, na bado hampati kwa sababu hamumwombi Mungu.
3 Mnaomba na hampokei kwa sababu mnaomba kwa ajili ya mambo mabaya, ili
kwamba muweze kuvitumia kwa tamaa zenu mbaya. 4 Enyi wazinzi! Hamjui
kwamba urafiki na ulimwengu ni uadui dhidi ya Mungu? Kwa hiyo, yeyote aamuaye
kuwa rafiki wa ulimwengu hujifanya mwenyewe adui wa Mungu. 5 Au mnadhani
maandiko hayana maana yasemapo kwamba Roho aliyoweka ndani yetu ana wivu
sana kwa ajili yetu? 6 Lakini Mungu hutoa neema zaidi, ndiyo maana maandiko
husema, “Mungu humpinga mwenye kiburi, lakini humpa neema mnyenyekevu.”
7 Hivyo, jitoeni kwa Mungu. Mpingeni ibilisi na yeye atakimbia kutoka kwenu.
8 Sogeeni karibu na Mungu, na yeye atakaribia karibu nanyi. Safisheni mikono yenu,
enyi wenye dhambi, na takaseni mioyo yenu, enyi wenye nia mbili. 9 Huzunikeni,
ombolezeni, na kuria! Geuzeni kicheko chenu kuwa huzuni na furaha yenu kuwa
maombolezo. 10 Jinyenyekezeni wenyewe mbele za Bwana, na atawainua juu.
11 Msineneane kinyume ninyi kwa ninyi, ndugu. Mtu anenaye kinyume na ndugu
yake, au kumhukumu ndugu yake, hunena kinyume na sheria na huihukumu sheria
ya Mungu. Mkiihukumu sheria, hamuitii sheria, bali mnaihukumu. 12 Ni mmoja tu
ambaye ni mtoa sheria na hakimu, Mungu, yeye ambaye ana uwezo wa kuokoa na
kuangamiza. Wewe ni nani ambaye unamhukumu jirani yako? 13 Sikilizeni, ninyi
msemao, “Leo au kesho tutakwenda katika mji huu, na kukaa mwaka huko, na
kufanya biashara, na kutengeneza faida.” 14 Ni nani ajuaye nini kitatokea kesho,
na maisha yenu ni nini hasa? Kwa kuwa mnafanana kama ukungu unaotokea kwa
muda mfupi na kisha hupotea. 15 Badala yake mngesema, “kama ni mapenzi ya
Bwana, tutaishi na tutafanya hiki au kile.” 16 Lakini sasa mnajivuna juu ya mipango
yenu. Majivuno yote hayo ni uovu. 17 Kwahiyo, kwake yeye ajuaye kutenda mema
lakini hayatendi, kwake huyo ni dhambi.

# 5

1 Njoni sasa, enyi mlio matajiri, lieni kwa sauti ya juu kwa sababu ya taabu
inayokuja juu yenu. 2 Utajiri wenu umeharibiwa na mavazi yenu yametafunwa na
wadudu waharibifu. 3 Dhahabu zenu na fedha zenu zimekosa thamani, na uharibifu
wake utashuhudia dhidi yenu na kuangamiza miili yenu kama moto. Mmejiwekea

hazina yenu katika siku za mwisho. 4 Tazameni, malipo ya watendakazi-wale ambao
hamjawalipa kwa kuvuna katika mashamba yenu- wanalia! Na kilio cha wale
waliovuna mazao yenu kimeyafikia masikio ya Bwana wa Majeshi. 5 Mmeishi kwa
anasa duniani na kujifurahisha ninyi wenyewe. Mmejinenepesha mioyo yenu kwa
siku ya machinjo. 6 Mmemhukumu na kumuua mwenye haki asiyeweza kuwapinga.
7 Kwa hiyo vumilieni, ndugu, mpaka ujio wa Bwana, kama mkulima husubiri mavuno
ya thamani toka katika nchi, akisubiri kwa uvumilivu kwa ajili yake, mpaka mvua za
kwanza na zile za mwisho zikinyesha. 8 Pia ninyi muwe wavumilivu; kazeni mioyo
yenu, kwa sababu kuja kwake Bwana ni karibu. 9 Ndugu, msinung'unikiane ninyi kwa
ninyi, kusudi msije mkahukumiwa. Tazama, hakimu anasimama mlangoni. 10 Kwa
mfano, ndugu, angalieni mateso na uvumilivu wa manabii walionena katika jina
la Bwana. 11 Tazama, twawaita wale wanaovumilia, “heri.” Mmesikia uvumilivu
wa Ayubu, na mnalijua kusudi la Bwana kwa ajili ya Ayubu, ni kwa jinsi gani
Bwana amejaa huruma na rehema. 12 Zaidi ya yote, ndugu zangu, msiape, aidha
kwa mbingu ama kwa nchi, au kwa kiapo cha aina nyingine. Bali hebu “ndiyo”
yenu na imaanishe “ndiyo” na “hapana” yenu na imaanishe “hapana,” ili kwamba
msije kuangukia chini ya hukumu. 13 Kuna yeyote miongoni mwenu ana mateso?
Lazima aombe. Je, mtu yeyote ni mwenye kuchangamka? Na aimbe sifa. 14 Je,
kuna yeyote miongoni mwenu aliye mgonjwa? Na awaite wazee wa kanisa, nao
wazee wa kanisa waombe juu yake, wakimpaka mafuta katika jina la Bwana, 15 na
maombi ya imani yatamponya mgonjwa, na Bwana atamwinua. Na kama atakuwa
ametenda dhambi, Mungu atamsamehe. 16 Kwa hiyo ungameni dhambi zenu ninyi
kwa ninyi, na kuombeana kila mmoja na mwenzake, ili muweze kuponywa. Maombi
ya mwenye haki huzaa matokeo makubwa. 17 Eliya alikuwa mtu mwenye hisia kama
zetu, aliomba kwa juhudi kwamba mvua isinyeshe, na haikunyesha katika nchi kwa
muda wa miaka mitatu na miezi sita. 18 Na Eliya aliomba tena, na mbingu zilimwaga
mvua juu ya nchi na nchi ikatoa mavuno. 19 Ndugu zangu, kama yeyote miongoni
mwenu anapotoka kutoka kwenye ukweli, lakini mtu mwingine akamrejesha, 20 hebu
na ajue kuwa yeyote amwongozaye mwenye dhambi kuondoka katika njia yake ya
ukosaji ataponya nafsi yake kutoka katika mauti na atafunika wingi wa dhambi.

# 1 Petro

[1] Petro, mtume wa Yesu Kristo, kwa wageni wa utawanyiko, kwa wateule, katika
Ponto yote, Galatia, Kapadokia, Asia, na Bithinia, [2] kutokana na ufahamu wa
Mungu, Baba, kwa kutakaswa na Roho Mtakatifu, kwa utiifu wa Yesu Kristo, na
kwa kunyunyuziwa damu yake. Neema iwe kwenu, na amani yenu iongezeke.
[3] Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo na abarikiwe. Katika ukuu wa rehema
yake, alitupa kuzaliwa upya kwa ujasiri wa urithi kupitia ufufuo wa Yesu Kristo
kutoka katika wafu, [4] kwa urithi usioangamia, hautakua na uchafu wala kupungua.
Umehihifadhiwa mbinguni kwa ajili yenu. [5] Kwa uwezo wa Mungu mnalindwa
kupitia imani kwa wokovu ambao upo tayari kufunuliwa katika nyakati za mwisho.
[6] Furahini katika hili, ingawaje sasa ni lazima kwenu kujisikia huzuni katika majaribu
ya aina mbalimbali. [7] Hii, ni kwa sababu imani yenu iweze kujaribiwa, imani ambayo
ni ya thamani kuliko dhahabu, ambayo inapotea katika moto ambao hujaribu imani
yenu. Hii hutokea ili imani yenu ipate kuzaa sifa, utukufu, na heshima katika ufunuo
wa Yesu Kristo. [8] Hamjamuona yeye, lakini mnampenda. Hamumuoni sasa, lakini
mnaamini katika yeye na mna furaha isiyoweza kuelezeka kwa furaha ambayo
imejawa na utukufu. [9] Sasa mnapokea wenyewe matokeo ya imani yenu, wokovu
wa nafsi zenu. [10] Manabii walitafuta na kuuliza kwa umakini kuhusu wokovu huu,
kuhusu neema ambayo ingekuwa yenu. [11] Walitafuta kujua ni aina gani ya wokovu
ambao ungekuja. Walitafuta pia kujua ni muda gani Roho wa Kristo aliye ndani yao
alikuwa anazungumza nini nao. Hii ilikua inatokea wakati alipokuwa anawaambia
mapema kuhusu mateso ya Kristo na utukufu ambao ungemfuata. [12] Ilifunuliwa kwa
manabii kwamba walikua wanayatumikia mambo haya, na si kwa ajili yao wenyewe,
bali kwa ajili yenu - masimulizi ya mambo haya kupitia wale wanaoleta injili kwenu
kwa njia ya Roho Mtakatifu aliyetumwa kutoka mbinguni, mambo ambayo hata
malaika wanatamani kufunuliwa kwake. [13] Kwa hiyo fungeni viuno vya akili zenu.
Muwe watulivu katika fikra zenu. Muwe na ujasiri mkamilifu katika neema ambayo
italetwa kwenu wakati wa kufunuliwa kwa Yesu Kristo. [14] Kama watoto watiifu,
msifungwe wenyewe na tamaa ambazo mlizifuata wakati mlipokua hamna ufahamu.
[15] Lakini kama vile aliyewaita alivyo mtakatifu, nanyi, pia, muwe watakatifu katika
tabia yenu yote maishani. [16] Kwa kuwa imeandkwa, “Iweni watakatifu, kwa
sababu Mimi ni mtakatifu.” [17] Na kama mkiita “Baba” yule ahukumuye kwa haki
kulingana na kazi ya kila mtu, tumia muda wa safari yako katika unyenyekevu.
[18] Mnafahamu kwamba haikuwa kwa fedha au dhahabu - vitu vinavyoharibika-
ambavyo mmekombolewa kutoka kwenye tabia zenu za ujinga ambazo mlijifunza
kutoka kwa baba zenu. [19] Lakini mmekombolewa kwa damu ya heshima ya Kristo,
kama ya kondoo asiye na hila wala doa. [20] Kristo alichaguliwa kabla ya misingi
ya dunia, lakini sasa siku hizi za mwisho, amefunuliwa kwenu. [21] Mnamwamini
Mungu kupitia yeye, ambaye Mungu alimfufua toka kwa wafu na ambaye alimpa
utukufu ili kwamba imani yenu na ujasiri uwe katika Mungu. [22] Mmefanya nafsi
zenu kuwa safi kwa utii wa ile kweli, kwa dhumuni la pendo la kidugu lililo na
unyofu, hivyo pendaneni kwa bidii toka moyoni. [23] Mmekwisha zaliwa mara ya pili,
si kwa mbegu iharibikayo, lakini kutoka katika mbegu isiyoharibika, kupitia uzima
na neno la Mungu lililosalia. [24] Kwa maana “ miili yote ni kama majani, na utukufu
wake wote ni kama ua la jani. Jani hunyauka, na ua hudondoka, [25] lakini neno la
Bwana hubakia milele.” Huu ni ujumbe ambao ulitangazwa kama injili kwenu.

# 2

1 Kwa hiyo wekeni pembeni uovu wote, udanganyifu, unafiki, wivu na kashifa.
2 Kama watoto wachanga, mtamani maziwa safi ya kiroho, ili kwamba mweze kukua
ndani ya wokovu, 3 kama mmeonja kwamba Bwana ni mwema. 4 Njoni kwake
aliye jiwe hai linaloishi ambalo limekataliwa na watu, lakini hilo limechaguliwa na
Mungu na ni la thamani kwake. 5 Ninyi pia ni kama mawe yaliyo hai yanayojengwa
juu kuwa nyumba ya kiroho, ili kuwa ukuhani mtakatifu ambao hutoa dhabihu
za kiroho zinazokubaliwa kwa Mungu kupitia Yesu Kristo. 6 Andiko husema hivi,
“Tazama, nimeweka katika Sayuni jiwe la pembeni, kuu na lililochaguliwa na la
thamani. Yeyote aaminiye katika yeye hataona aibu”. 7 Hivyo heshima ni yenu
kwenu ninyi mnaoamini. Lakini, “jiwe lililokataliwa na wajenzi, hili limekuwa jiwe
kuu la pembeni”- 8 na, “jiwe la kujikwaa na mwamba wa kujikwaa.”Wao hujikwaa,
wanaolikataa neno, kwa lile ambalo pia walikuwa wameteuliwa kwalo. 9 Lakini
ninyi ni ukoo uliochaguliwa, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa miliki ya
Mungu, ili kwamba mweze kutangaza matendo ya ajabu ya yule aliyewaita kutoka
gizani kuja kwenye nuru yake ya ajabu. 10 Ninyi kwanza hamkuwa watu, lakini
sasa ninyi ni watu wa Mungu. Ninyi hamkupokea rehema, lakini sasa mmepokea
rehema. 11 Wapendwa, nimewaita kama wageni na wazurujaji kujinyima kutoka
kwenye tamaa mbaya za dhambi, ambazo zinapigana vita na roho zenu. 12 Mnapaswa
kuwa na tabia njema kati ya mataifa, ili kwamba, kama watawasema kama kwamba
mmefanya mambo maovu, wataziangalia kazi zenu njema na kumsifu Mungu katika
siku ya kuja kwake. 13 Tii kila mamlaka ya mwanadamu kwa ajili ya Bwana,
ikiwa mfalme kama mkuu, 14 ikiwa watawala waliotumwa kuwaadhibu watenda
mabaya na kuwasifu wale wanaotenda mema. 15 Kwa kuwa ni mapenzi ya Mungu,
kwamba kwa kufanya mema mwanyamazisha mazungumzo ya kipuuzi ya watu
wapumbavu. 16 Kama watu huru, msiutumie uhuru wenu kama kifuniko kwa maovu,
bali muwe kama watumishi wa Mungu. 17 Waheshimuni watu wote. Wapendeni
ndugu. Mwogopeni Mungu. Mweshimuni mfalme. 18 Watumwa, watiini bwana
zenu kwa heshima yote, siyo tu bwana walio wazuri na wapole, lakini pia walio
waovu. 19 Kwa kuwa ni sifa kama yeyote atavumilia maumivu wakati anapoteseka
pasipo haki kwa sababu ya dhamiri yake kwa Mungu. 20 Ni faida gani iliyopo kama
mwadumu kutenda dhambi kisha mwendelee kuadhibiwa? Lakini kama mmefanya
mema na ndipo mteseke kwa kuhukumiwa, hii ni sifa njema kwa Mungu. 21 Kwa
hili mliitwa, kwa sababu Kristo pia aliteswa kwa ajili yenu, amewaachia mfano
kwa ajili yenu kufuata nyayo zake. 22 Yeye hakufanya dhambi, wala haukuonekana
udanganyifu wowote kinywani mwake. 23 Wakati yeye alipotukanwa, hakurudisha
matukano, alipoteseka, hakutisha bali alijitoa mwenyewe kwake Yeye ahukumuye
kwa haki. 24 Yeye mwenyewe alizibeba dhambi zetu katika mwili wake kwenye mti,
ili kwamba tusiwe na sehemu tena katika dhambi, na kwamba tuishi kwa ajili ya
haki. Kwa kupigwa kwake ninyi mmepona. 25 Wote mliokuwa mkitangatanga kama
kondoo aliyepotea, lakini sasa mmerudi kwa mchungaji na mlinzi wa roho zenu.

# 3

1 Kwa njia hii, ninyi ambao ni wake mnapaswa kujitoa kwa waume zenu wenyewe,
ili, hata kama baadhi yao hawajalitii neno, kupitia tabia za wake zao wanaweza
kuvutwa pasipo neno, 2 kwa sababu wao wenyewe watakuwa wameiona tabia yenu
njema pamoja na heshima. 3 Hii ifanyike siyo kwa mapambo ya nje—kusuka nywele,
vito vya dhahabu, au mavazi ya mtindo. 4 Lakini badala yake ifanyike kwa utu wa
ndani wa moyo, na kuzidi katika uzuri wa unyenyekevu na utulivu wa moyo, ambao
ni wa thamani mbele za Mungu. 5 Kwa kuwa wanawake watakatifu walijipamba

wenyewe kwa njia hii. Walikuwa na imani katika Mungu na waliwatii waume
zao wenyewe. [6] Kwa njia hii Sara alimtii Ibrahamu na kumwita yeye “bwana”
wake. Ninyi sasa ni watoto wake kama mtafanya yaliyo mazuri na kama hamwogopi
mabaya. [7] Kwa njia hiyo hiyo, ninyi wanaume mnapaswa kuishi na wake zenu
mkijua kuwa wao ni wenzi wa kike dhaifu, mkiwatambua wao kama wapokeaji
wenzenu wa zawadi ya uzima. Fanyeni hivi ili kwamba maombi yenu yasizuiliwe.
[8] Hatimaye, ninyi nyote, muwe na nia moja, wenye huruma, upendo kama ndugu,
wanyenyekevu, na wapole. [9] Msilipe ovu kwa ovu, au tusi kwa tusi. Kinyume chake,
mwendelee kubariki, kwa sababu hii mliitwa, ili kwamba muweze kurithi baraka.
[10] “Yeye atakaye kupenda maisha na kuona siku njema lazima auzuie ulimi wake kwa
mabaya na midomo yake kusema hila. [11] Na ageuke na kuacha mabaya na kufanya
yaliyo mazuri. Atafute amani na kuifuata. [12] Macho ya Bwana humwona mwenye
haki na masikio yake husikia maombi yake. Lakini uso wa Bwana uko kinyume
cha wale watendao uovu.” [13] Ni nani atakayewadhuru ninyi, ikiwa mwatamani lililo
zuri? [14] Lakini kama mkiteseka kwa haki, mmebarikiwa. Msiogope yale ambayo wao
wanayaogopa. Msiwe na wasiwasi. [15] Badala yake, mmuweke Kristo Bwana katika
mioyo yenu kama mtakatifu. Kila mara muwe tayari kumjibu kila mtu anayewauliza
ninyi kwa nini mna tumaini katika Mungu. Fanyeni hivi kwa upole na heshima.
[16] Muwe na dhamiri njema ili kwamba watu wanaotukana maisha yenu mema katika
Kristo waweze kuaibika kwa sababu wanaongea kinyume dhidi yenu kama kwamba
mlikuwa watenda maovu. [17] Ni vizuri zaidi, ikiwa Mungu anatamani, kwamba
mwateseka kwa kufanya mema kuliko kwa kufanya mabaya. [18] Kristo pia aliteseka
mara moja kwa ajili ya dhambi. Yeye ambaye ni mwenye haki aliteseka kwa ajili
yetu, ambao hatukuwa wenye haki, ili kwamba atulete sisi kwa Mungu. Alikufa
katika mwili, lakini alifanywa mzima katika roho. [19] Katika roho, alikwenda na
kuzihubiri roho ambazo sasa ziko kifungoni. [20] Hazikuwa tiifu wakati uvumilivu wa
Mungu ulipokuwa unasubiri wakati wa Nuhu, siku za ujenzi wa safina, na Mungu
aliokoa watu wachache—nafsi nane—kutoka katika maji. [21] Hii ni alama ya ubatizo
unaowaokoa ninyi sasa, siyo kama kuosha uchafu kutoka mwilini, lakini kama ombi
la dhamiri njema kwa Mungu, kupitia ufufuo wa Yesu Kristo. [22] Yeye yuko mkono wa
kuume wa Mungu. Alikwenda mbinguni. Malaika, mamlaka, na nguvu lazima vimtii
yeye.

# 4

[1] Kwa hiyo, kwa kuwa Kristo aliteseka katika mwili, jivikeni silaha za nia ile
ile. Yeye aliyeteseka katika mwili ameondokana na dhambi. [2] Mtu huyu haendelei
tena kuishi katika tamaa za mwili, bali kwa mapenzi ya Mungu, kwa maisha yake
yaliyosalia. [3] Kwa kuwa muda uliopita umetosha kutenda mambo ambayo wamataifa
wanataka kufanya- ufisadi, nia mbaya, ulevi, ulafi, sherehe za kipagani na ibada za
sanamu zenye machukizo. [4] Wanafikiri ni ajabu mnapojiepusha kutenda mambo
hayo pamoja nao, hivyo wananena maovu juu yenu. [5] Watatoa hesabu kwake aliye
tayari kuhukumu walio hai na wafu. [6] Kwa kusudi hili injili ilihubiriwa kwao
waliokwisha kufa, kwamba ijapokuwa walikwisha hukumiwa katika miili yao kama
wanadamu, ili waweze kuishi kulingana na Mungu katika roho. [7] Mwisho wa mambo
yote unakuja. Kwa hiyo, mwe na ufahamu ulio sahihi, na iweni na nia njema kwa
ajili ya maombi yenu. [8] Kabla ya mambo yote, eweni na bidii katika upendo kwa
kila mmoja, kwa kuwa upendo hautafuti kufunua dhambi za wengine. [9] Onyesheni
ukarimu kwa kila mmoja bila kunung'unika. [10] Kama ambavyo kila mmoja wenu
alivyopokea karama, itumieni katika kuhudumiana, kama wasimamizi wema wa
karama nyingi zilizotolewa bure na Mungu. [11] Kama mtu akiongea, na iwe kama

mausia ya Mungu, na kama mtu akihudumu, na iwe kama uwezo aliopewa na Mungu,
ili kwamba kwa kila jambo Mungu apate kutukuzwa kupitia Yesu Kristo. Utukufu na
uweza vina Yeye milele na milele. Amina. [12] Wapendwa, msihesabu jaribu ambalo
huja kuwajaribu kama kitu kigeni, ingawa kuna kitu kigeni kilichokuwa kinatukia
kwenu. [13] Lakini kwa kadri mnavyozidi kupata uzoefu wa mateso ya Kristo, furahini,
ili kwamba mfurahi pia na kushangilia katika ufunuo wa utukufu wake. [14] Iwapo
mmetukanwa kwa ajili ya jina la Kristo, mmebarikiwa, kwa sababu ya Roho wa
utukufu na Roho wa Mungu anakaa juu yenu. [15] Lakini asiwepo yeyote mwenye
kuteswa kama muuaji, mwizi, mtenda maovu, au ajishughulishaye na mambo ya
wengine. [16] Lakini ikiwa mtu anateswa kama Mkristo, asione aibu, bali amtukuze
Mungu katika jina hilo. [17] Kwa kuwa wakati umefika kwa hukumu kuanzia katika
nyumba ya Mungu. Na kama inaanzia kwetu, itakuwaje kwa wale wasioitii injili ya
Mungu? [18] Na kama “mwenye haki anaokolewa kupitia magumu, itakuwaje kwa mtu
asiyehaki na mwenye dhambi?” [19] Kwa hiyo wote wanaoteseka kutokana na mapenzi
ya Mungu wakabidhi nafsi zao kwa Muumba mwaminifu ili hali wakitenda mema.

# 5

[1] Ninawasihi wazee waliomo miongoni mwenu, mimi, niliye mzee mwenzao na
shahidi wa mateso ya Kristo, na ambaye vile vile ni mshirika katika utukufu
utakaodhihirika. [2] Kwa hiyo, ninawatia moyo ninyi wazee, lichungeni kundi la
Mungu lililo miongoni mwenu. Liangalieni, sio kwa sababu mnapaswa, lakini kwa
sababu mnatamani hivyo, kulingana na Mungu. Liaangalieni, sio kwa kupenda
pesa za aibu, lakini kwa kupenda. [3] Msijifanye mabwana juu ya watu waliyochini
ya uangalizi wenu, lakini iweni mfano katika kundi. [4] Pale Mchungaji Mkuu
atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu isiyopoteza uthamani wake. [5] Vilevile,
nanyi vijana wadogo, nyenyekeni kwa wakubwa wenu. Ninyi nyote, uvaeni
unyenyekevu na kuhudumiana ninyi kwa ninyi, kwani Mungu huwapinga wenye
kiburi, lakini huwapa neema wanyenyekevu. [6] Kwa hiyo nyenyekeni chini ya mkono
wa Mungu uliyo hodari ili kwamba awainue kwa wakati wake. [7] Mwekeeni fadhaa
zenu juu yake, kwa sababu anawajali. [8] Iweni na busara, iweni waangalifu. Yule
adui yenu, ibilisi, kama simba aungurumaye ananyatia, akisaka mtu wa kumrarua.
[9] Simameni kinyume chake. Kuweni na nguvu katika imani yenu. Mkijua kwamba
ndugu zenu walioko ulimwenguni wanapitia mateso kama hayo. [10] Baada ya kuteseka
kwa muda kitambo, Mungu wa neema yote, aliyewaita katika utukufu wa milele
ndani ya Kristo, atawakamilisha, atawaimarisha na kuwatia nguvu. [11] Enzi iwe
kwake milele na milele. Amina. [12] Namthamini Silwano kama ndugu mwaminifu, na
nimewaandikia ninyi kwa ufupi kupitia kwake. Ninawatia moyo na ninashuhudia
kwamba nilichokiandika ni neema ya kweli ya Mungu. Simameni ndani yake.
[13] Waamini waliloko Babeli, waliochaguliwa pamoja nanyi, wanawasalimu, na Marko
mwanangu, anawasalimu. [14] Salimianeni kila mmoja kwa busu la upendo. Na amani
iwe kwenu mliondani ya Kristo.

# 2 Petro

1 Simon Petro, Mtumwa na Mtume wa Yesu Kristo, Kwa wale walioipokea imani
ile ile ya thamani kama tulivyoipokea sisi, imani iliyo ndani ya haki ya Mungu na
mwokozi wetu Yesu Kristo. 2 Neema iwe kwenu; amani iongezeke kupitia maarifa
ya Mungu na Bwana wetu Yesu. 3 Kupitia maarifa ya Mungu tumepata mambo yake
yote kwa ajili ya uchaji wamaisha, Toka kwa Mungu aliyetuita kwa ajili ya uzuri
wa utukufu wake. 4 Kwa njia hii alitutumainishia ahadi kuu za thamani. Alifanya
hili ili kutufanya warith wa asili ya Mungu, kwa kadiri tunavyoendelea kuuacha
uovu wa dunia hii. 5 Kwa sababu hii, fanyeni bidii kuongeza uzuri kwa njia ya
imani yenu, kwa sababu ya uzuri, maarifa. 6 Kupitia maarifa, kiasi, na kupitia kiasi
saburi, na kupitia saburi, utauwa. 7 Kupitia utauwa upendo wa ndugu na kupitia
upendo wa ndugu, upendo. 8 Kama mambo haya yamo ndani yenu, yakiendelea
kukua ndani yenu, basi ninyi hamtakuwa tasa au watu msiozaa matunda katika
maarifa ya Bwana wetu Yesu Kristo. 9 Lakini yeyote asiyekuwa na mambo haya,
huyaona mambo ya karibu tu; yeye ni kipofu. amesahau utakaso wa dhambi zake
za kale. 10 Kwa hiyo, ndugu zangu, fanyeni juhudi ili kujihakikishia uteule na wito
kwa ajili yenu. Kama mtayafanya haya, hamtajikwaa. 11 Hivyo mtajipatia wingi wa
lango la kuingilia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu na mwokozi Yesu Kristo.
12 Kwa hiyo mimi nitakuwa tayari kuwakumbusha mambo haya kila mara, hata kama
mnayafahamu, na sasa mmekuwa imara katika kweli. 13 Nafikiria kuwa niko sahihi
kuwaamsha na kuwakumbusha juu ya mambo haya, ningali nimo katika hema hii.
14 Kwa maana najua kuwa si muda mrefu nitaiondoa hema yangu, kama Bwana Yesu
Kristo alivyonionyesha. 15 Nitajitahidi kwa bidii kwa ajili yenu ili mkumbuke mambo
haya baada ya mimi kuondoka. 16 Kwa kuwa sisi hatukufuata hadthi zilizoingizwa
kwa ustadi pale tulipowaeleza juu ya nguvu na kujidhihirisha kwa Bwana wetu Yesu
Kristo, bali sisi tulikuwa mashahidi wa utukufu wake. 17 Yeye alipokea Utukufu
na heshima toka kwa Mungu baba pale sauti iliposikika toka katika utukufu mkuu
ikisema, “Huyu ndiye mwanangu, mpendwa wangu ambaye nimependezwa naye.”
18 Tuliisikia sauti hii ikitokea mbinguni pale tulipokuwa naye kwenye ule mlima
mtakatifu. 19 Tunalo hili neno la unabii lililothibitika, ambalo kwalo mwafanya
vyema kulitekeleza. Ni kama taa ing'aayo gizani mpaka kuchapo na nyota za
mawio zionekanazo katika mioyo yenu. 20 Tambueni haya ya kwamba, hakuna
unabii unaoandikwa kwa sababu ya kujifikirisha kwa nabii mwenyewe. 21 Kwa
kuwa hakuna unabii uliokuja kwa mapenzi ya mwanadamu, isipokuwa wanadamu
waliwezeshwa na Roho Mtakatifu aliyeongea toka kwa Mungu.

## 2

1 Manabii wa uongo walijitokeza kwa Waisraeli, na walimu wa uongo watakuja
pia kwenu. Kwa siri wataleta mafundisho ya uongo nao watamkana Bwana
aliyewanunua. Wanajiletea uharibifu wa haraka juu yao wenyewe. 2 Wengi
watafuata njia zao za aibu na kupitia wao wataikufuru njia ya ukweli. 3 Kwa uchoyo
watawanyonya watu wakitumia maneno ya uongo Hukumu yao haitachelewa,
uharibifu utawafuata. 4 Maana Mungu hakuwaacha malaika waliokengeuka. Bali
aliwatupa kuzimu ili wafungwe minyororo mpaka hukumu itakapowajilia. 5 Wala
Mungu hakuuvumilia ulimwengu wa zamani. Bali, alimhifadhi Nuhu, mwenye wito
wa haki, pamoja na wengine saba, wakati alipoachila gharika juu ya ulimwengu
ulioasi. 6 Mungu aliihukumu miji ya Sodoma na Gomora kiasi cha kuwa majivu

na uharibifu ili iwe mfano kwa ajili ya waovu katika siku za usoni 7 Lakini
alipofanya hilo, alimwokoa Lutu mtu wa haki, aliyekuwa amehuzunishwa na tabia
chafu za wasiofuata sheria za Mungu. 8 Kwa kuwa huyo mtu wa haki, aliyeishi
nao siku kwa siku akiitesa nafsi yake kwa ajili ya yale aliyoyasikia na kuyaona.
9 Kwa hiyo Bwana anajua jinsi ya kuwaokoa watu wake wakati wa mateso na
jinsi ya kuwavumilia waovu kwa ajili ya hukumu katika siku ya mwisho. 10 Kwa
hakika huu ndio ukweli kwa wale wanoendelea kuishi katika tamaa za mwili huu
na kuyadharau mamlaka. Watu wa jinsi hii wana ujasiri katika dhamiri zao,
Hawaogopi kuwakufuru watukufu. 11 Ingawa malaika wana uwezo na nguvu kuliko
wanadamu, lakini hawawezi kuleta hukumu dhidi yao kwa Bwana 12 Lakini hawa
wanyama wasio na akili wametengenezwa kwa asili ya kukamatwa na kuangamizwa.
13 Wanaumizwa kwa ujira wa maovu yao. Mchana kutwa huishi kwa anasa. Wamejaa
uchafu na maovu. Hufurahia anasa za udanganyifu wanaposherehekea na wewe.
14 Macho yao yamefunikwa na uzinzi; hawatosheki kutenda dhambi. Huwalaghai
na kuwaangusha waumini wachanga katika dhambi. Wana mioyo iliyojaa tamaa,
ni watoto waliolaaniwa. 15 Wameiacha njia ya kweli. wamepotoka na wameifuata
njia ya Balaam mwana wa Beori, aliyependa kupata malipo ya udhalimu. 16 Lakini
alikemewa kwa ajili ya ukosai wake. Punda aliyekuwa bubu akiongea katika sauti
ya binadamu, alizuia wazimu wa nabii.. 17 Watu hawa ni kama chemichemi zisizo
na maji. Ni kama mawingu yanayotoweshwa na upepo. Wingu zito limehifadhiwa
kwa ajili yao. 18 Huongea kwa majivuno matupu. Huwaangusha watu kwa tamaa
ya mwili. Huwalaghai watu wanaojaribu kuwakimbia wale waishio katika ukosaji.
19 Huwaahidi watu uhuru wakati wao wenyewe ni watumwa wa dhambi ya ufisadi.
Maana mwanadamu hufanywa kuwa mtumwa wa kile kinachomtawala. 20 Yeye
ajiepushaye na uchafu wa ulimwengu kwa kutumia maarifa ya Bwana na mwokozi
Yesu Kristo, na kisha akarudia uchafu huo tena, hali yake huwa mbaya kuliko ile ya
mwanzo. 21 Ingefaa watu hao kama wasingeifahamu njia ya haki kuliko kuifahamu
na kisha tena kuziacha amri takatifu walizopewa. 22 Mithali hii huwa na ukweli kwao.
“mbwa huyarudia matapishi yake. Na nguruwe aliyeoshwa hurudi tena kwenye
matope.”

# 3

1 Ssa, ninakuandikia wewe, mpendwa hii barua ya pili ili kukuamsha katika akili,
2 ili kwamba uweze kukumbuka maneno yaliyosemwa kabla na manabii watakatifu
na kuhusu amri ya Bwana wetu na mwokozi kwa kutumia mitume. 3 Ujue ili kwanza,
kwamba wasaliti watakuja katika siku za mwisho kuwasaliti ninyi, wakienenda
sawasawa na matakwa yao. 4 Na wakisema “Iko wapi ahadi ya kurudi? Baba zetu
walikufa, Lakini vitu vyote vilikuwa hivyo tangu mwanzo wa uumbaji. 5 Wakajifanya
kusahau kwamba nchi na mbingu vilianza kutokana na maji na kupitia maji zamani
za kale, kwa neno la Mungu, 6 na kwamba kupitia neno lake na maji yakawa
ulimwengu kwa kipindi hicho, ikiwa imejaa maji, iliharibiwa. 7 Lakini sasa mbingu
na dunia zimetunzwa kwa neno hilo hilo kwa ajili ya moto. Vimehifadhiwa kwa ajili
ya siku ya hukumu na maangamizi ya watu wasio wa Mungu 8 Hii haiwezi kuchenga
ujumbe wako, wapendwa, kwamba siku moja kwa bwana ni kama miaka elfu moja.
Na miaka elfu moja ni kama siku moja. 9 Si kwamba Bwana anafanya pole pole
kutimiza ahadi, kama inavyofikiriwa kuwa, Lakini yeye ni mvumilivu kwa ajili yenu,
yeye hatamani hata mmoja aangamie, Lakini hutamani kutoa muda ili wote wapate
kutubu. 10 Ingawa, siku ya Bwana itakuja kama mwizi, mbingu itapita kwa kupaza
kelele. Vitu vitateketezwa kwa moto. Nchi na vitu vyote vilivyomo vitafunuliwa wazi.
11 Kwa kuwa vitu vyote vutateketezwa kwa njia hii. Je utakuwa mtu wa aina gani?

Uishi kitakatifu na maisha ya kimungu. 12 Inakupasa kujua na kutambua haraka ujio
wa siku ya Mungu. Siku hiyo mbingu itateketezwa kwa moto. Na vitu vitayeyushwa
katika joto kali. 13 Lakini kutokana na ahadi yake, tunasubiri mbingu mpya na nchi
mpya, ambapo wenye haki wataishi 14 Hivyo wapendwa kwa kuwa tunatarajia vitu
hivi, jitahidi kuwa makini na kutolaumika na kuwa na amani pamoja naye. 15 Na
zingatia uvumilivu wa Bwana wetu katika wokovu, kama mpendwa kaka yetu Paulo,
alivyowaandikia ninyi, kutokana na hekima ambayo alipewa. 16 Paulo anaongelea
hayo yote katika barua zake, kuna vitu ambavyo ni vigumu kuvielewa. Watu
wasio na adabu na uimara wameviharibu vitu hivyo, Na kama wanavyofanya kwa
maandiko. Kuelekea maangamizi yao. 17 Hivyo, wapendwa kwa kuwa mnayafahamu
hayo. Jilindeni wenyewe ili kwamba msipotoshwe na udanganyifu wa walaghai na
kupoteza uaminifu. 18 Lakini mkue katika neema na ufahamu wa Bwana na mwokozi
Yesu Kristo. Na sasa utukufu una yeye sasa na milele. Amina.

# 1Yohana 1

1 Kile kilichokuwapo tangu mwanzo-kile tulichokisikia, kile tulichokiona kwa
macho yetu, kile tulichokitazama, na mikono yetu imekishika-kuhusu Neno la uzima.
2 Na ule uzima ulifanywa kujulikana wazi, na tumeuona, na kuushuhudia, na
kuwatangazia uzima wa milele, ambao ulikuwa kwa Baba na ulifanywa kujulikana
kwetu. 3 Kile tulichokiona na kukisikia twakitangaza kwenu pia, ili kwamba muweze
kujumuika pamoja nasi, na ushirika wetu pamoja na Baba na Mwanae Yesu Kristo.
4 Na tunawandikia mambo haya ninyi ili kwamba furaha yetu iwe timilifu. 5 Huu ndio
ujumbe tuliousikia kutoka kwake na kuwatangazia: Mungu ni nuru na ndani yake
hakuna giza hata kidogo. 6 Kama tukisema kwamba tunaushirika naye na twatembea
gizani, twadanganya na hatutendi kweli. 7 Lakini tukitembea katika nuru kama alivyo
katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu ya Yesu Kristo, mwanae yatutakasa
kutoka dhambi zote. 8 Kama tukisema hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, na
kweli haimo ndani yetu. 9 Lakini tukizitubu dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na
haki kutusamehe dhambi zetu na kututakasa na uovu wote. 10 Tukisema kwamba
hatujatenda dhambi, twamfanya yeye kuwa muongo, na neno lake halimo ndani
yetu.

## 2

1 Watoto wangu wapendwa, nawaandikia mambo haya kwenu ili msitende dhambi.
Lakini kama mmoja wenu akitenda dhambi, tunaye wakili aliye pamoja na Baba,
Yesu Kristo- ambaye ni mwenye haki. 2 Yeye ni mpatanishi kwa dhambi zetu, na si
kwa dhambi zetu pekee, lakini pia kwa ulimwengu mzima. 3 Kwa hili twajua kwamba
twamjua yeye, kama tukizitunza amri zake. 4 Yeye asemaye, “Namjua Mungu,” lakini
hazishiki amri zake, ni mwongo, na kweli haimo ndani yake. 5 Lakini yeyote ashikaye
neno lake, kweli katika mtu yule upendo wa Mungu umekamilishwa. Katika hili
twajua kwamba tuko ndani yake. 6 Yeye asemaye anaishi ndani ya Mungu anapaswa
mwenyewe pia kuenenda kama vile Yesu Kristo alivyoenenda. 7 Wapenzi, siwaandikii
ninyi amri mpya, bali amri ya zamani ambayo mmekwisha kuwa nayo tangu
mwanzo. Amri ya zamani ni neno ambalo mlilolisikia. 8 Hata hivyo ninawaandikia
ninyi amri mpya, ambayo ni kweli katika Kristo na kwenu, kwa sababu giza linapita,
na nuru ya kweli iko tayari inaangaza 9 Yeye asemeye yuko kwenye nuru na amchukia
ndugu yake yuko katika giza hata sasa. 10 Yeye ampendaye ndugu yake anaishi katika
nuru na hakuna jambo lolote liwezalo kumkwaza. 11 Lakini yeye amchukiaye ndugu
yake yuko gizani na anatembea gizani; Yeye hajui wapi aendako, kwa sababu giza
limeyapofusha macho yake. 12 Nawaandikia ninyi, watoto wapendwa, kwa sababu
mmesamehewa dhambi zenu kwa ajili ya jina lake. 13 Nawaandikia ninyi, akina
baba, kwa sababu mnamjua yeye aliye tangu mwanzo. Nawaandikia ninyi, vijana,
kwa sababu mmemshinda yule mwovu. Nimewaandikia ninyi, watoto wadogo, kwa
sababu mnamjua Baba. 14 Nimewaandikia ninyi, akina baba, kwa sababu mnamjua
yeye aliye tangu mwanzo. Nimewaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mko imara,
na neno la Mungu linakaa ndani yenu, na mmemshinda yule mwovu. 15 Msiipende
dunia wala mambo ambayo yaliyo katika dunia. Iwapo yule ataipenda dunia, upendo
wa kumpenda Baba haumo ndani yake. 16 Kwani kila kitu kilichomo katika dunia-
tamaa ya mwili, tamaa ya macho, na kiburi cha uzima- havitokani na Baba lakini
vinatokana na dunia. 17 Dunia na tamaa zake zinapita. Bali yeye afanyaye mapenzi ya
Mungu huyo adumu milele. 18 Watoto wadogo, ni wakati wa mwisho. Kama ambavyo
mmesikia kwamba mpinga kristo anakuja, hata sasa wapinga kristo wamekuja, kwa

hali hii tunajua kwamba ni wakati wa mwisho. [19] Walikwenda zao kutoka kwetu,
kwani hawakuwa wa kwetu. Kama vile wangekuwa wa kwetu wangeendelea kuwa
pamoja nasi. Lakini wakati walipo kwenda zao, hicho kilionyesha hawakuwa wa
kwetu. [20] Lakini mumetiwa mafuta na yule Mtakatifu, nanyi nyote mnaijua kweli.
[21] Sikuwaandikia ninyi kwa sababu hamuijui kweli, bali kwa sababu mnaijua na
kwa sababu hakuna uongo wa ile kweli [22] Nani ni mwongo bali ni yeye anayepinga
kwamba Yesu ni Kristo? Huyu mtu ni mpinga kristo, pale anapo mpinga Baba na
Mwana. [23] Hakuna anaye mpinga Mwana akawa na Baba. Yeyote anaye mkiri
Mwana anaye Baba pia. [24] Kama kwa ajili yenu, kile mlichosikia toka mwanzo acha
kiendelee kuwa ndani yenu. Kama kile mlichosikia toka mwanzo kitakaa ndani
yenu, pia, mtakaa ndani ya Mwana na Baba. [25] Na hii ni ahadi aliyotupatia sisi:
uzima wa milele. [26] Nimewaandikia haya ninyi kuhusu wale ambao wangewaongoza
ninyi katika upotevu. [27] Na kwa ajili yenu, yale mafuta mliyoyapokea kutoka kwake
yanakaa ndani yenu, na hamtahitaji mtu yeyote kuwafundisha. bali kama mafuta
yake yanawafundisha kuhusu mambo yote na ni kweli na siyo uongo, na hata kama
yameshawafundisha, kaeni ndani yake. [28] Na sasa, watoto wapendwa, kaeni ndani
yake, ili wakati atakapotokea, tuweze kuwa na ujasiri na siyo kujisikia aibu mbele
yake katika kuja kwake. [29] Kama mnajua kuwa yeye ni mwenye haki, mnajua
kwamba kila mmoja atendaye haki amezaliwa na yeye.

# 3

[1] Oneni ni pendo la namna gani ametupatia Baba, kwamba tunaitwa watoto wa
Mungu, na hivi ndivyo tulivyo. Kwa sababu hii ulimwengu hautumtambui kwa kuwa
haukumtambua yeye. [2] Wapendwa sisi sasa ni watoto wa Mungu, na haijadhihirika
bado jinsi tutakavyokuwa. Twajua kwamba Kristo atakapoonekana, tutafanana
naye, kwani tutamuona kama alivyo. [3] Na kila mmoja ambaye ana ujasiri huu
kuhusu wakati ujao ulioelekezwa kwake, hujitakasa mwenyewe kama yeye alivyo
mtakatifu. [4] Kila mtu anayeendelea kutenda dhambi huvunja sheria. Kwa sababu
dhambi ni uvunjaji sheria. [5] Mnajua Kristo alidhihilishwa ili kuziondoa dhambi
kabisa. Na ndani yake hamna dhambi. [6] Hakuna hata mmoja adumue ndani
yake na kuendelea kutenda dhambi. Hakuna mtu hata mmoja adumuye katika
dhambi ikiwa amemuona au kumfahamu yeye. [7] Watoto wapendwa, msikubali
kupotoshwa na mtu yeyote. Atendaye haki ni mwenye haki, kama vile Kristo naye
alivyo mwenye haki. [8] Atendaye dhambi ni wa ibilisi, kwa sababu ibilisi ni mtenda
dhambi tangu mwanzo. Kwa sababu hii Mwana wa Mungu alidhihilishwa ili aweze
kuziharibu kazi za ibilisi. [9] Yeyote aliyezaliwa na Mungu hatendi dhambi, kwa
sababu mbegu ya Mungu hukaa ndani yake. Hawezi kuendelea kutenda dhambi
kwa sababu amezaliwa na Mungu. [10] Katika hili watoto wa Mungu na watoto wa
ibilisi wanafahamika. Yeyote asiyetenda kilicho cha haki, siyo wa Mungu, wala yule
ambaye hawezi kumpenda ndugu yake. [11] Kwani huu ndio ujumbe mliousikia kutoka
mwanzo, kwamba tunapaswa kupendana sisi kwa sisi, [12] siyo kama Kaini ambaye
alikuwa wa mwovu na alimuua ndugu yake. Na kwa nini alimuua? Kwa sababu
matendo yake yalikuwa maovu, na yale ya ndugu yake yalikuwa ya haki. [13] Ndugu
zangu, msishangae, endapo ulimwengu utawachukia. [14] Twajua tumekwisha toka
mautini na kuingia uzimani, kwa sababu tunawapenda ndugu. Yeyote ambaye hana
upendo hudumu katika mauti. [15] Mtu yeyote anaye mchukia ndugu yake ni muuaji.
Na mnajua kuwa uzima wa milele haukai ndani ya muuaji. [16] Katika hili tunalijua
pendo, kwa sababu kristo aliutoa uhai wake kwa ajili yetu. Nasi yatupasa kuyatoa
maisha yetu kwa ajili ya ndugu. [17] Lakini yeyote aliye na vitu, na anamuona ndugu
yake mwenye uhitaji, lakini huuzuia moyo wake wa huruma kwa ajili yake; je,

upendo wa Mungu unakaaje ndani yake? 18 Watoto wangu wapenzi, tusipende kwa
midomo wala kwa maneno matupu bali katika vitendo na kweli. 19 Katika hili tunajua
kwamba sisi tuko katika kweli, na mioyo yetu inathibitika katika yeye. 20 Ikiwa kama
mioyo yetu yatuhukumu, Mungu ni mkuu kuliko mioyo yetu, na yeye hujua mambo
yote. 21 Wapenzi, kama mioyo yetu haituhukumu, tunao ujasiri kwa Mungu. 22 Na
chochote tuombacho tutakipokea kutoka kwake, kwa sababu tunazishika amri zake
na tunafanya mambo yanayopendeza mbele zake. 23 Na hii ndiyo amri yake- ya
kwamba yatupasa kuamini katika jina la Mwanaye Yesu Kristo na kupendana sisi
kwa sisi-kama alivyotupatia amri yake. 24 Anayezitii amri zake hudumu ndani yake,
na Mungu hukaa ndani yake. Na kwa sababu hii twajua kuwa hukaa ndani yetu,
Kwa yule Roho aliyetupa.

# 4

1 Wapendwa, msiiamini kila roho, lakini zijaribuni roho muone kama zinatokana
na Mungu, kwa sababu manabii wengi wa uongo wametokea duniani. 2 Kwa hili
mtamjua Roho wa Mungu - kila roho itakayokiri kuwa Yesu Kristo amekuja katika
mwili ni ya Mungu, 3 na kila roho isiyomkiri Yesu si ya Mungu. Hii ni roho ya mpinga
kristo, ambayo mliyoisikia kuwa inakuja, na sasa tayari iko duniani. 4 Ninyi ni wa
Mungu, watoto wapendwa, na mmekwisha washinda kwa sababu yeye aliye ndani
yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika ulimwengu. 5 Wao ni wa ulimwengu, kwa hiyo
wanachokisema ni cha ulimwengu, na ulimwengu unawasikiliza. 6 Sisi ni wa Mungu.
Yeye amjuaye Mungu hutusikiliza sisi. Yeye asiye wa Mungu hawezi kutusikiliza.
Katika hili tunajua roho wa kweli na roho wa uongo. 7 Wapendwa, tupendane sisi
kwa sisi, kwa vile upendo ni wa Mungu, na kila mmoja apendaye amezaliwa na
Mungu na kumjua Mungu. 8 Yeye asiyependa hamjui Mungu, kwa sababu Mungu
ni upendo. 9 Katika hili pendo la Mungu lilifunuliwa miongoni mwetu, kwamba
Mungu alimtuma Mwanae wa pekee ulimwenguni ili tuishi kupitia yeye. 10 Katika
hili pendo, si kwamba tulimpenda Mungu, lakini yeye alitupenda, na akamtuma
Mwanawe awe fidia ya dhambi zetu. 11 Wapendwa, ikiwa Mungu alitupenda sisi,
vile vile tunapaswa kupendana sisi kwa sisi. 12 Hakuna hata mmoja aliyemuona
Mungu. Kama tukipendana sisi kwa sisi, Mungu anakaa ndani yetu na pendo lake
limekamilika ndani yetu. 13 Katika hili tunajua kuwa tunakaa ndani yake na yeye
ndani yetu, kwa sababu ametupa Roho wake. 14 Na tumeona na kushuhudia kuwa
Baba amemtuma Mwana kuwa mwokozi wa ulimwengu. 15 Kila anayekiri kwamba
Yesu ni Mwana wa Mungu, Mungu anakaa ndani yake na yeye ndani ya Mungu.
16 Na tunajua na kuamini upendo alio nao Mungu ndani yetu. Mungu ni pendo, na
yeye anayekaa ndani ya upendo anakaa ndani ya Mungu, na Mungu hukaa ndani
yake. 17 Katika pendo hili limekwisha kamilishwa kati yetu, ili tuwe na ujasiri siku
ya hukumu, kwa sababu kama yeye alivyo, na sisi ndivyo tulivyo katika ulimwenngu
huu. 18 Hakuna hofu ndani ya pendo. Lakini pendo kamili huitupa hofu nje, kwa
sababu hofu huhusiana na hukumu. Lakini yeye aogopaye hajakamilishwa katika
pendo. 19 Tunapenda kwa sababu Mungu alitupenda kwanza. 20 Ikiwa mmoja
atasema, “Nampenda Mungu” lakini anamchukia ndugu yake, ni mwongo. Kwa
sababu asiyempenda ndugu yake, anayemuona, hawezi kumpenda Mungu ambaye
hajamuona. 21 Na hii ndiyo amri tuliyo nayo kutoka kwake: Yeyote ampendaye
Mungu, anapaswa kumpenda ndugu yake pia.

# 5

1 Yeyote anayeamini kuwa Yesu ni Kristo amezaliwa na Mungu. Na yeyote
ampendaye yeye ambaye ametoka kwa Baba pia huwapenda watoto wake. 2 Kwa

hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu — tunapompenda Mungu na
kutekeleza amri zake. 3 Hivi ndivyo tunavyompenda Mungu kwamba twazishika
amri zake. Na amri zake ni nyepesi. 4 Kwa kuwa kila aliyezaliwa na Mungu
huushinda ulimwengu. Na huu ndio ushindi wa kuushinda ulimwengu, imani yetu.
5 Ni nani aliyeushinda ulimwengu? Ni yule aaminiye kwamba Yesu ni Mwana wa
Mungu. 6 Huyu ndiye aliyekuja kwa maji na damu- Yesu Kristo. Hakuja tu kwa
maji bali kwa maji na damu. 7 Kwa kuwa kuna watatu washuhudiao: 8 Roho,
maji na damu. Hawa watatu hukubaliana. (Zingatia: Maneno haya “Baba, Neno,
na Roho Mtakatifu” hayaonekani katika nakala bora za kale). 9 Kama tunaupokea
ushuhuda wa wanadamu ushuhuda wa Mungu ni mkuu kuliko huo. Kwa kuwa
ushuhuda wa Mungu ni huu- kwamba anao ushuhuda kuhusiana na Mwanawe.
10 Yeye amwaminiye Mwana wa Mungu ana ushuhuda ndani yake mwenyewe. Na
yeyote asiye mwamini Mungu amemfanya kuwa mwongo, kwa kuwa hakuuamini
ushuhuda ambao Mungu ameuleta kuhusu Mwanawe. 11 Na ushuhuda ndio huu —
kwamba Mungu alitupa uzima wa milele, na uzima huu umo ndani ya Mwanawe.
12 Aliye naye Mwana ana uzima. Asiyekuwa naye Mwana wa Mungu hana uzima.
13 Nimewaandikia haya mweze kujua kwamba mnao uzima wa milele — ninyi
mnaoamini katika jina la Mwana wa Mungu. 14 Na huu ndio ujasiri tulionao mbele
zake, kwamba kama tukiomba kitu chochote sawa sawa na mapenzi yake, hutusikia.
15 Na kama tunajua kwamba hutusikia — chochote tumwombacho tunajua kwamba
tunacho hicho tulichomwomba. 16 Kama mtu amwonaye ndugu yake anatenda
dhambi isiyopelekea kifo, yampasa kuomba na Mungu atampa uzima. Ninasema kwa
wale ambao dhambi yao ni ile isiyopelekea kifo — Kuna dhambi ipelekeayo kifo —
sisemi kwamba anapaswa kuomba kwa ajilli ya dhambi hiyo. 17 Uasi wote ni dhambi
— lakini kuna dhambi isiyopelekea kifo. 18 Tunajua ya kuwa aliyezaliwa na Mungu
hatendi dhambi. Bali aliyezaliwa na Mungu hutunzwa naye salama daima, na yule
mwovu hawezi kumdhuru. 19 Tunajua kuwa sisi ni wa Mungu na tunajua kwamba
ulimwengu wote uko chini ya utawala wa yule mwovu. 20 Lakini twajua kwamba
Mwana wa Mungu amekuja na ametupatia ujuzi, kwamba tunamjua yeye aliye kweli
na kwamba tumo ndani yake yeye aliye kweli, hata katika Mwanawe Yesu Kristo. Ni
Mungu wa kweli na uzima wa milele. 21 Watoto wapenzi, jiepusheni na sanamu.

# 2 Yohana

[1] Kutoka kwa mzee kwenda kwa mwanamke mteule na watoto wake, ambao
niwapendao katika kweli na si mimi tu, bali na wote wale wanao ifahamu kweli, [2] kwa
sababu ya kweli iliyomo ndani yetu na itakayodumu pamoja nasi milele. [3] Neema,
rehema, amani zitakuwa nasi kutoka kwa Mungu Baba na kutoka kwa Yesu Kristo,
Mwana wa Baba, katika kweli na pendo. [4] Ninafurahi sana kwamba nimegundua
baadhi ya watoto wanaenenda katika kweli, kama vile tu tulivyoipokea amri hii
kutoka kwa Baba. [5] Na sasa nakusihi wewe, mwanamke, siyo kwamba nakuandikia
amri mpya, bali ile tuliyokuwa nayo tokea mwanzo, kwamba tunapaswa kupendana
sisi kwa sisi. Na huu ndiyo upendo, tunaopaswa kuenenda, kulingana na amri yake.
[6] Hii ndiyo ile amri, kama mlivyoisikia tokea mwanzo, kwamba mnapaswa kuenenda
katika hiyo. [7] Kwa kuwa wadanganyifu wengi wamesambaa katika ulimwengu, na
hawakiri kwamba Yesu Kristo alikuja katika mwili. Huyu ndiye mdanganyifu na
mpinga Kristo. [8] Jiangalieni wenyewe kwamba hampotezi mambo yale tuliyokwisha
fanyia kazi, lakini ili kwamba mweze kuipokea tuzo kamili. [9] Yeyote aendeleae
mbele na hadumu katika fundisho la Kristo, hana Mungu. Yeye adumuye katika
fundisho anaye Baba na Mwana pia. [10] Kama mtu anakuja kwenu na haleti fundisho
hili, msimkaribishe katika nyumba zenu na msimsalimie. [11] Kwa kuwa amsalimuye
hushiriki katika matendo yake maovu. [12] Ninayo mambo mengi ya kukuandikia, na
sikutaka kuyaandika kwa karatasi na wino. Lakini natumaini kuja kwenu na kuongea
uso kwa uso, kwamba furaha yetu ipate kufanywa kamili. [13] Watoto wa dada yenu
mteule wanawasalimia.

# 3 Yohana

1 Mzee, kwa Gayo mpenzi, ninayempenda katika kweli. 2 Mpendwa, nakuombea
ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya njema, kama vile roho yako
inavyofanikiwa. 3 Maana nilifurahi sana wakati nilipoambiwa na ndugu waliokuja
na kutoa ushuhuda juu ya kweli yako, kama vile unavyoenenda katika kweli. 4 Sina
furaha kubwa zaidi ya hii, kusikia kwamba watoto wangu wanatembea katika
kweli. 5 Mpendwa, unaenenda kwa uaminifu unapowahudumia ndugu na wageni,
6 ambao wametoa ushuhuda wa upendo wako mbele ya kanisa. Unafanya vizuri
kuwasafirisha katika safari zao kwa namna ambayo inampendeza Mungu. 7 Kwa
sababu kwa ajili ya Jina, walienda bila kuchukua kitu chochote kutoka kwa watu wa
Mataifa. 8 Hivyo, tunatakiwa kuwakaribisha watu kama hawa, ili tuwe watenda kazi
wenza kwa ajili ya kweli. 9 Nililiandikia kusanyiko jambo fulani, lakini Diotrofe,
anayependa kuwa wa kwanza miongoni mwao, hakubaliani na sisi. 10 Hivyo,
kama nikija nitayakumbuka matendo yake anayoyafanya, jinsi anavyosema maneno
mabaya kinyume nasi. Hajaridhika na matendo haya, yeye mwenyewe hawapokei
ndugu. Hata huwakataza wengine ambao wanatamani kuwakaribisha hao ndugu
na kuwafukuza watoke kwenye kusanyiko. 11 Mpenzi, usiige kilicho kibaya, bali
iga kilicho chema. Yeye atendaye mema ni wa Mungu; na yeye atendaye mabaya
hajamwona Mungu. 12 Demetrio ameshuhudiwa na wote na kweli yenyewe. sisi pia
ni mashahidi, na unajua kuwa ushahuhuda wetu ni wa kweli. 13 Ninayo mambo
mengi ya kukuandikia, lakini sipendi kukuandikia kwa kalamu na wino. 14 Bali
ninatarajia kukuona hivi karibuni, na tutaongea nawe ana kwa ana. 15 Amani iwe
pamoja nawe. Marafiki wanakusalimu. Wasalimu marafiki kila mmoja kwa jina lake.

# Yuda

[1] Yuda, mtumwa wa Yesu Kristo, na ndugu yake Yakobo, kwa wale ambao
wameitwa, wapendwao katika Mungu Baba, na waliotunzwa kwa ajili ya Yesu Kristo:
[2] rehema na amani na upendo viongezwe kwenu. [3] Wapenzi, wakati nilipokuwa
nikifanya kila juhudi kuwaandikia ninyi kuhusu wokovu wetu sote, ilinilazimu
kuwaandikia kwa ajili ya kuwashauri ili mshindanie kwa uaminifu imani ambayo
ilikuwa imekabidhiwa mara moja tu kwa waamini. [4] Kwa sababu watu fulani
wamejiingiza kwa siri kati yenu - watu ambao walitiwa alama kwa ajili ya hukumu
- watu wasio wataua ambao hubadili neema ya Mungu wetu kuwa ufisadi, na
kumkana Bwana wetu pekee na Bwana Yesu Kristo. [5] Sasa napenda kuwakumbusha
ninyi ingawa kuna wakati mlijua kwa ukamilifu kwamba Bwana aliwaokoa watu
kutoka nchi ya Misri, lakini baadaye kuwaangamiza wale ambao hawakuamini.
[6] Na malaika ambao hawakuilinda enzi yao wenyewe lakini wakaacha makao yao
maalum Mungu amewaweka katika minyororo ya milele, ndani ya giza, kwa ajili
ya hukumu ya siku ile kuu. [7] Kama vile Sodoma na Gomora na miji iliyoizunguka,
ambayo pia ilijiingiza yenyewe katika uasherati na wakafuata tamaa isiyo ya asili.
Walioneshwa kama mifano ya wale ambao huteseka katika hukumu ya moto wa
milele. [8] Hali kadhalika, kwa njia ile ile waota ndoto hawa pia huchafua miili
yao, na hukataa mamlaka, na wananena uongo dhidi ya mtukufu. [9] Lakini hata
Mikaeli malaika mkuu, wakati alipokuwa akishindana na ibilisi na kuhojiana naye
kwa ajili ya mwili wa Musa, hakuthubutu kuleta hukumu ya uongo dhidi yake,
lakini badala yake alisema, “Bwana akukemee!” [10] Lakini watu hawa huleta uongo
dhidi ya chochote wasicho kifahamu. Na kile wasicho kifahamu- kile ambacho
wanyama wasio na akili hujua kwa silika- haya ndiyo yaliyo waharibu. [11] Ole
wao! Kwa kuwa wametembea katika njia ya Kaini, na kulifuata kosa la Balaamu.
Wameangamia katika uasi wa Kora. [12] Hawa ni miamba katika sherehe zenu za
upendo, wakisherehekea bila aibu, wakijilisha tu wenyewe. Ni mawingu yasiyo na
maji, yanayobebwa na upepo, ni miti iliyopukutika isiyo na matunda iliyo kufa mara
mbili, iliyong'olewa mizizi [13] Ni mawimbi ya bahari yenye kelele yakitoa aibu yao
wenyewe, Ni nyota zinazorandaranda ambazo weusi wa giza umetunzwa kwa ajili
yao milele. [14] Enoko, wa saba katika orodha ya Adamu, alitabiri kuhusu wao, akisema,
“Tazama! Bwana anakuja na maelfu kwa maelfu ya watakatifu wake, [15] ili afanye
hukumu juu ya kila mtu, na kutia hatia wote wasiomcha Mungu juu ya matendo yao
yote waliyokwishafanya katika njia zisizo za kitauwa, na kwa maneno yote ya ukali
ambayo wasio watauwa wameyanena dhidi yake.” [16] Hawa ni wale wanung'unikao,
walalamikao ambao hufuata tamaa zao za uovu, wajivunao mno, ambao kwa faida
yao hudanganya wengine. [17] Lakini ninyi, wapenzi, kumbukeni maneno ambayo
yalinenwa zamani na mitume wa Bwana Yesu Kristo. [18] Walisema kwenu, “Katika
wakati wa mwisho kutakuwa na watu wanaodhihaki ambao hufuata tamaa zao zisizo
za kitauwa.” [19] Watu hawa ni watenganishaji, wanatawaliwa na tamaa za asili, na
hawana Roho. [20] Lakini ninyi, wapenzi, kama mjijengavyo katika imani yenu takatifu
sana, na kama muombavyo katika Roho Mtakatifu, [21] jitunzeni katika upendo wa
Mungu, na msubiri rehema ya Bwana wetu Yesu Kristo ambayo huwapatia uzima
wa milele. [22] Onesheni rehema kwa wale walio na shaka. [23] Waokoeni wengine
kwa kuwanyakua kutoka katika moto. Kwa wengine onesheni huruma kwa hofu,
mkichukia hata vazi lililotiwa doa na mwili. [24] Sasa kwake awezaye kuwalinda
msijikwae, na kuwasababisha msimame mbele ya utukufu wake, bila mawaa na

kuwa na furaha kuu, 25 kwake Mungu pekee mwokozi kupitia Yesu Kristo Bwana
wetu, utukufu uwe kwake, ukuu, uwezo na nguvu kabla ya nyakati zote, na sasa na
hata milele. Amina.

# Ufunuo

1 Huu ni ufunuo wa Yesu Kristo ambao Mungu alimpa ili kuwaonesha watumishi
wake mambo ambayo lazima yatokee karibuni. Aliyafanya yajulikane kwa kumtuma
malaika wake kwa mtumishi wake Yohana. 2 Yohana alitoa ushuhuda wa kila
kitu alichoona kuhusiana na neno la Mungu na kwa ushuhuda uliotolewa kuhusu
Yesu Kristo. 3 Amebarikiwa yeye asomaye kwa sauti na wale wote wanaoyasikia
maneno ya unabii huu na kutii kilichoandikwa humo, kwa sababu muda umekaribia.
4 Yohana, kwa makanisa saba yaliyoko Asia: neema iwe kwenu na amani kutoka
kwake aliyepo, aliyekuwepo, na atakayekuja, na kutoka kwa roho saba walio mbele
ya kiti chake cha enzi, 5 na kutoka kwa Yesu Kristo ambaye ni shahidi mwaminifu,
mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, na mtawala wa wafalme wa dunia hii. Kwake
yeye atupendaye na ametuweka huru kutoka katika dhambi zetu kwa damu yake,
6 ametufanya kuwa ufalme, makuhani wa Mungu na Baba yake - kwake kuwa
utukufu na nguvu milele daima. Amina. 7 Tazama, anakuja na mawingu; kila jicho
litamwona, pamoja na wote waliomchoma. Na kabila zote za dunia wataomboleza
kwake. Ndiyo, Amina. 8 “Mimi ni Alfa na Omega,” asema Bwana Mungu, “Yeye
aliyepo, na aliyekuwepo, na ambaye anakuja, Mwenye nguvu.” 9 Mimi, Yohana
- ndugu yenu na mmoja anayeshiriki pamoja nanyi katika mateso na ufalme na
uvumilivu thabiti ulio katika Yesu; nilikuwa katika kisiwa kiitwacho Patimo kwa
sababu ya neno la Mungu na ushuhuda kuhusu Yesu. 10 Nilikuwa katika Roho siku ya
Bwana. Nilisikia nyuma yangu sauti ya juu kama ya tarumbeta, 11 ikisema, “andika
katika kitabu unayo yaona, na uyatume kwa makanisa saba, kwenda Efeso, kwenda
Smirna, kwenda Pergamo, kwenda Thiatira, kwenda Sardi, kwenda Philadelphia, na
kwenda Laodikia.” 12 Nikageuka kuona ni sauti ya nani aliyekuwa akiongea nami,
na nilipogeuka niliona kinara cha dhahabu cha taa saba. 13 Katikati ya kinara cha
taa alikuwemo mmoja kama Mwana wa Adamu, amevaa kanzu ndefu iliyofika chini
ya miguu yake, na mkanda wa dhababu kuzunguka kifua chake. 14 Kichwa chake
na nywele zake zilikuwa nyeupe kama sufu nyeupe kama theluji, na macho yake
yalikuwa kama mwali wa moto. 15 Nyayo zake zilikuwa kama shaba iliyosuguliwa
sana, kama shaba ambayo imekwisha pitishwa katika moto, na sauti yake ilikuwa
kama sauti ya maji mengi yanayotiririka kwa kasi. 16 Alikuwa ameshikilia nyota
saba katika mkono wake wa kuume, na kutoka kinywani mwake kulikuwa na upanga
mkali wenye makali kuwili. Uso wake ulikuwa uking'aa kama mwanga mkali wa jua.
17 Nilipomwona, nikaanguka miguuni pake kama mtu aliyekufa. Akaweka mkono
wake wa kulia juu yangu na kusema, “Usiogope! Mimi ni wa kwanza na wa Mwisho,
18 na ambaye ninaishi. Nalikuwa nimekufa, lakini tazama, ninaishi milele! Na ninazo
funguo za mauti na kuzimu. 19 Kwa hiyo, yaandike uliyoyaona, yaliyopo sasa, na
yale yatakayotokea baada ya haya. 20 Kwa maana iliyojificha kuhusu nyota saba
ulizoziona katika mkono wangu wa kuume, na kile kinara cha dhahabu cha taa saba:
nyota saba ni malaika wa yale makanisa saba, na kinara cha taa saba ni yale makanisa
saba.”

## 2

1 “Kwa malaika wa kanisa la Efeso andika: 'Haya ni maneno ya yule anayeshikilia
zile nyota saba katika mkono wake wa kuume. Yeye atembeaye kati ya vinara vya
dhahabu vya taa saba asema hivi, “ 2 '“Najua ambacho umetenda na bidii yako ya
kazi na uvumilivu wako thabiti, na kwamba huwezi kuhusiana nao walio waovu,
na umewajaribu wote wanaojiita kuwa mitume na kumbe siyo, na wameonekana

kuwa waongo. 3 Najua una subira na uvumilivu, na umepitia mengi kwa sababu ya
jina langu, na haujachoka bado. 4 Lakini hili ndilo nililonalo dhidi yako, umeuacha
upendo wako wa kwanza. 5 Kwa hiyo kumbuka ulipoanguka, ukatubu na kufanya
matendo uliyofanya tangu mwanzo. Usipotubu, nitakuja kwako na kukiondoa kinara
chako kutoka mahali pake. 6 Lakini wewe una hili, unachukia yale ambayo Wanikolai
wameyatenda, ambayo hata mimi nayachukia. 7 Kama una sikio, sikiliza yale ambayo
Roho anayaambia makanisa. Na kwa yeye ashindaye nitampa kibali cha kula kutoka
katika mti wa uzima ulio katika paradiso ya Mungu.' 8 “Kwa malaika wa kanisa la
Smirna andika: 'Haya ni maneno ya yule ambaye ni mwanzo na mwisho ambaye
alikufa na kuwa hai tena: 9 '“Nayajua mateso yako na umasikini wako (lakini
wewe ni tajiri), na uongo wa wale wanaojiita ni wayahudi (lakini siyo - wao ni
sinagogi la Shetani). 10 Usiogope mateso yatakayokupata. Tazama! Ibilisi anataka
kuwatupa baadhi yenu gerezani ili mpate kujaribiwa, na mtateseka kwa siku kumi.
Iweni waaminifu hadi kufa, na nitawapa taji ya uzima. 11 Kama una sikio, sikiliza
Roho anavyoyaambia makanisa. Yeye ashindaye hatapata madhara ya mauti ya
pili.' 12 “Kwa malaika wa kanisa la Pergamo andika: 'Haya ndiyo anenayo yeye
aliye nao huo upanga mkali, wenye makali kuwili. 13 '“Najua mahali unapoishi
-mahali kilipo kiti cha enzi cha shetani. Hata hivyo wewe walishika sana jina
langu, na hukuikana imani yako iliyo kwangu, hata siku zile za Antipasi shahidi
wangu, mwaminifu wangu, aliyeuawa miongoni mwenu, hapo ndipo Shetani anaishi.
14 Lakini nina mambo machache dhidi yako: unao huko watu washikao mafundisho
ya Balaamu, yeye aliyemfundisha Balaki kuweka vikwazo mbele ya wana wa Israel,
ili wale vyakula vilivyotolewa sadaka kwa miungu na kuzini. 15 Katika hali iyo hiyo,
hata wewe unao baadhi yao wanaoshika mafundisho ya Wanikolai. 16 Basi tubu!
Na usipofanya hivyo, naja upesi, na nitafanya vita dhidi yao kwa upanga utokao
katika kinywa changu. 17 Kama una sikio, sikiliza Roho anachowaambia makanisa.
Yeye ashindaye, nitampa baadhi ya ile mana iliyofichwa, pia nitampa jiwe jeupe
lililoandikwa jina jipya juu ya jiwe, jina ambalo hakuna alijuaye isipokuwa yeye
alipokeaye.' 18 “Kwa malaika wa kanisa la Thiatira andika: “Haya ndiyo maneno
ya Mwana wa Mungu, yeye aliye na macho yake kama mwali wa moto, na nyayo
kama shaba iliyosuguliwa sana: 19 '“Najua ambacho umefanya - upendo wako na
imani na huduma na uvumilivu wako thabiti, na kwamba kile ulichofanya hivi
karibuni ni zaidi ya kile ulichofanya mwanzo. 20 Lakini ninalo hili dhidi yako:
unamvumilia mwanamke Yezebeli anayejiita mwenyewe nabii mke. Kwa mafundisho
yake, anawapotosha watumishi wangu kuzini na kula chakula kilichotolewa sadaka
kwa sanamu. 21 Nilimpa muda wa kutubu, lakini hayuko tayari kuutubia uovu wake.
22 Angalia! Nitamtupa kwenye kitanda cha maradhi, na wale watendao uasherati
naye kwenye mateso makali, vinginevyo watubu kwa alichofanya. 23 Nitawapiga
wanawe wafe na makanisa yote watajua kwamba mimi ndiye niyachunguzaye
mawazo na tamaa. Nitampa kila mmoja wenu kadiri ya matendo yake. 24 Lakini
kwa baadhi yenu mliosalia katika Thiatira, kwa wale wote msioshika fundisho
hili, na msiojua kile ambacho baadhi huita mafumbo ya Shetani, nasema kwenu,
'sitaweka juu yenu mzigo wowote.' 25 Kwa jambo lolote, lazima muwe imara mpaka
nitakapokuja. 26 Yeyote ashindaye na kufanya kile nilichofanya hadi mwisho, kwake
yeye nitampa mamlaka juu ya mataifa. 27 'Atawatawala kwa fimbo ya chuma, kama
mabakuli ya udongo, atawavunja vipande vipande.' 28 Kama nilivyopokea kutoka
kwa Baba yangu, nitampa pia nyota ya asubuhi. 29 Ukiwa na sikio, sikiliza kile
ambacho Roho anayaambia makanisa.'

# 3

[1] Kwa malaika wa kanisa la Sardi andika: 'Maneno ya yule anayeshikilia zile
roho saba za Mungu na nyota saba. "Najua ambacho umefanya. Una sifa ya kuwa
hai, lakini u-mfu. [2] Amka na kuimarisha yaliyosalia, lakini yako karibu kufa, kwa
sababu sikuyaona matendo yako yamekamilika machoni pa Mungu wangu. [3] Kwa
hiyo, kumbuka, yale uliyoyapokea na kusikia. Yatii na kutubu. Lakini usipoamka,
nitakuja kama mwivi, na hutajua saa ipi nitakayokuja juu yako. [4] Lakini kuna
majina machache ya watu katika Sardi ambao hawakuchafua nguo zao. Watatembea
pamoja nami, wamevaa nguo nyeupe, kwa sababu wanastahili. [5] Yeye ashindaye
atavikwa mavazi meupe, na kamwe sitalifuta jina lake kutoka katika kitabu cha
uzima, na nitalitaja jina lake mbele ya Baba yangu, na mbele ya malaika. [6] Ukiwa na
sikio, sikiliza Roho ayaambiavyo makanisa." [7] "Kwa malaika wa kanisa la Philadefia
andika: Maneno ya aliye mtakatifu na kweli - aliye na funguo za Daudi, hufungua
na hakuna afungaye, hufunga na hakuna awezaye kufungua. [8] Najua ambacho
umetenda. Tazama, nimekuwekea mbele yako mlango uliofunguliwa ambao hakuna
awezaye kuufunga. Najua unazo nguvu kidogo, lakini umelitii neno langu na
hujalikana jina langu. [9] Angalia! Wote walio wa sinagogi la shetani, wale wasemao
wao ni Wayahudi na kumbe siyo, badala yake wanadanganya. Nitawafanya waje
na kusujudu mbele ya miguu yako, na watajua ya kuwa nilikupenda. [10] Kwa kuwa
umetunza amri yangu kwa uvumilivu wa uthabiti, nitakulinda pia katika saa yako ya
kujaribiwa ambayo inakuja katika ulimwengu wote, kuwajaribu wale wote wanaoishi
katika nchi. [11] Naja upesi. Shikilia sana kile ulichonacho ili asiwepo mtu wa kuitwaa
taji yako. [12] Nitamfanya yeye ashindaye kuwa nguzo katika hekalu la Mungu wangu,
na hatatoka nje kamwe. Nitaliandika kwake jina la Mungu wangu, jina la mji wa
Mungu wangu (Yerusalemu mpya, ushukao chini toka mbinguni kwa Mungu wangu),
na jina langu jipya. [13] Yeye aliye na sikio, na asikie ambacho Roho anasema kwa
makanisa.' [14] "Kwa malaika wa kanisa la Laodikia andika: 'Maneno yake aliye Amina,
wakutegemewa na shahidi mwaminifu, mtawala juu ya uumbaji wa Mungu. [15] Najua
ambacho umefanya, na kwamba wewe si baridi wala moto, natamani kwamba
ungekuwa wa baridi au moto! [16] Hivyo, kwa sababu wewe ni vuguvugu, si moto
wala baridi, nitakutapika utoke kinywani mwangu. [17] Kwa kuwa unasema, "Mimi
ni tajiri, nimekuwa na mali nyingi, na sihitaji chochote." Lakini hujui kwamba
wewe ni duni sana, wakuhuzunikiwa, maskini, kipofu na uchi. [18] Sikiliza ushauri
kwangu: Nunua kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto ili upate kuwa tajiri,
na nguo nyeupe za kumetameta ili ujivike mwenyewe na usioneshe aibu ya uchi
wako, na mafuta ya kupaka katika macho yako upate kuona. [19] Kila nimpendaye,
namwelekeza na kuwafundisha namna iwapasavyo kuishi; kwa hiyo, kuwa mkweli
na kutubu. [20] Tazama nasimama katika mlango na kubisha. Yeyote asikiaye sauti
yangu na kufungua mlango, nitakuja na kuingia nyumbani kwake, na kula chakula
naye na yeye pamoja nami. [21] Yeye ashindaye, nitampa haki ya kukaa chini pamoja
nami juu ya kiti changu cha enzi, kama vile mimi nilivyoshinda na kukaa chini
pamoja na Baba yangu juu ya kiti chake cha enzi. [22] Yeye aliye na sikio, na asikilize
ambacho Roho ayaambia makanisa."

# 4

[1] Baada ya mambo haya nilitazama, nikaona kuwa mlango ulikuwa umefunguliwa
mbinguni. Ile sauti ya kwanza, ikizungumza nami kama tarumbeta, ikisema, "Njoo
hapa, nitakuonesha yatakayotokea baada ya mambo haya." [2] Mara moja nilikuwa
katika Roho, niliona kulikuwa na kiti cha enzi kimewekwa mbinguni, na mtu
amekikalia. [3] Mmoja aliyekuwa amekikalia alionekana kama jiwe la yaspi na akiki.

Kulikuwa na upinde wa mvua umekizunguka kiti cha enzi. Upinde wa mvua
ulionekana kama zumaridi. 4 Kukizunguka kiti cha enzi kulikuwa na viti vya enzi
vingine ishirini na vinne, na waliokaa kwenye viti vya enzi walikuwa wazee ishirini
na wanne, wamevikwa mavazi meupe na taji za dhahabu vichwani mwao. 5 Kutoka
katika kiti cha enzi kulitoka miale ya radi, muungurumo na radi. Taa saba zilikuwa
zikiwaka mbele ya kiti cha enzi, taa ambazo ni roho saba za Mungu. 6 Tena mbele
ya kiti cha enzi kulikuwa na bahari, iliyowazi kama kioo. Wote kuzunguka kiti cha
enzi kulikuwa na wenye uhai wanne, waliojaa macho mbele na nyuma. 7 Kiumbe wa
kwanza mwenye uhai alikuwa kama simba, kiumbe wa pili mwenye uhai alikuwa
kama ndama, kiumbe wa tatu mwenye uhai alikuwa na uso kama wa mwanadamu,
na yule mwenye uhai wa nne alikuwa kama tai apaaye. 8 Viumbe wenye uhai wanne
kila mmoja alikuwa na mabawa sita, wamejaa macho juu na chini yake. Usiku
na mchana hawakomi kusema, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Bwana Mungu,
mtawala juu ya wote, aliyekuwepo, na aliyepo na atakayekuja." 9 Kila wakati viumbe
wenye uhai walipotoa utukufu, heshima, na kushukuru mbele za aliyekuwa ameketi
kwenye hicho kiti cha enzi, yeye aishiye milele na daima, 10 wazee ishirini na wanne
walisujudu wenyewe mbele yake aliyekikalia kiti cha enzi. Waliinama chini kwake
aishiye milele na daima na kutupa chini taji zao mbele ya kiti cha enzi wakisema,
11 "Wastahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kupokea utukufu na heshima
na nguvu. Kwa kuwa uliviumba vitu vyote, na kwa mapenzi yako, vilikuwepo na
viliumbwa."

# 5

1 Kisha nikaona katika mkono wa kulia wa yule aliyekuwa amekaa katika kiti
cha enzi, gombo lililoandikwa mbele na nyuma, na lilikuwa limetiwa mihuri saba.
2 Nilimwona malaika mwenye nguvu akihubiri kwa sauti kubwa, "Nani astahiliye
kulifungua gombo na kuzivunja mihuri yake?" 3 Hakuna mtu mbinguni au duniani
au chini ya dunia aliyeweza kulifungua gombo au kulisoma. 4 Nililia kwa uchungu
kwa kuwa hakupatikana yeyote aliyestahili kulifungua gombo au kulisoma. 5 Lakini
mmoja wa wazee akaniambia, "Usilie. Tazama! Simba wa kabila ya Yuda, shina la
Daudi, ameshinda, na anaweza kulifungua gombo na mihuri yake saba." 6 Kati ya
kiti cha enzi na wenye uhai wanne na miongoni mwa wazee, niliona mwanakondoo
amesimama, akionekana kama aliye uawa. Alikuwa na pembe saba na macho saba -
hizi ni roho saba za Mungu zilizotumwa duniani kote. 7 Akaenda akalichukua gombo
kutoka katika mkono wa kuume wa yule aliye kaa katika kiti cha enzi. 8 Alipolichukua
gombo, wenye uhai wanne na wazee ishirini na wanne wakainama hadi nchi mbele
ya mwanakondoo. Kila mmoja alikuwa na kinubi na bakuli ya dhahabu iliyojaa
uvumba ambayo ni maombi ya waamini. 9 Waliimba wimbo mpya: "Unastahili
kulitwaa gombo na kuzifungua muhuri zake. Kwa kuwa ulichinjwa, na kwa damu
yako ukamnunulia Mungu watu wa kila kabila, lugha, jamaa na taifa. 10 Ukawafanya
ufalme na makuhani kwa ajili ya kumtumikia Mungu wetu, nao watatawala juu ya
nchi." 11 Kisha nilitazama na nikasikia sauti ya malaika wengi kuzunguka kiti cha
enzi - idadi yao ilikuwa 200, 000, 000 na wenye uhai na wazee. 12 Wakasema kwa sauti
kuu, "Astahili mwanakondoo ambaye amechinjwa kupokea uwezo, utajiri, hekima,
nguvu, heshima, utukufu, na sifa." 13 Nikasikia kila kilichoumbwa kilichokuwa
mbinguni na duniani na chini ya nchi na juu ya bahari, kila kitu ndani yake kikisema,
"Kwake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi na kwa mwanakondoo, kuwe sifa, heshima,
utukufu na nguvu ya kutawala milele na milele." 14 Wenye uhai wanne wakasema,
"Amina!" na wazee wakainama chini na kuabudu.

# 6

1 Nikatazama wakati mwanakondoo alipofungua moja ya zile muhuri saba,
nikasikia mmoja wa wale wenye uhai wanne akisema kwa sauti iliyofanana na radi,
“Njoo!” 2 Nikatazama na palikuwa na farasi mweupe! Aliyempanda alikuwa na
bakuli, na akapewa taji. Alitokea kama mshindi ashindaye ili ashinde. 3 Wakati
mwanakondoo alipofungua muhuri wa pili, nikasikia mwenye uhai wa pili akisema,
“Njoo!” 4 Kisha farasi mwingine akatokea - mwekundu kama moto. Aliye mpanda
alipewa ruhusa ya kuondoa amani duniani, ili kwamba watu wachinjane. Huyu aliye
mpanda alipewa upanga mkubwa. 5 Wakati mwanakondoo alipofungua ule muhuri
wa tatu, nikasikia mwenye uhai wa tatu akisema, “Njoo!” Nikaona farasi mweusi, na
aliyempanda ana mizani mkononi mwake. 6 Nikasikia sauti iliyoonekana kuwa ya
mmoja wa wale wenye uhai ikisema, “kibaba cha ngano kwa dinari moja na vibaba
vitatu vya shayiri kwa dinari moja. Lakini usiyadhuru mafuta na divai.” 7 Wakati
mwanakondoo alipofungua muhuri ya nne, nilisikia sauti ya mwenye uhai wa nne
ikisema, “Njoo!” 8 Kisha nikaona farasi wa kijivu. Aliye mpanda aliitwa jina lake
mauti, na kuzimu ilikuwa ikimfuata. Walipewa mamlaka juu ya robo ya nchi, kuua
kwa upanga, kwa njaa na kwa ugonjwa, na kwa wanyama wa mwitu katika nchi.
9 Wakati mwanakondoo alipofungua muhuri ya tano, niliona chini ya madhabahu
roho za wale waliokuwa wameuawa kwa sababu ya neno la Mungu na kutokana
na ushuhuda walioushika kwa uthabiti. 10 Wakalia kwa sauti kuu, “mpaka lini,
Mtawala wa vyote, mtakatifu na mkweli, utahukumu wakaao juu ya nchi, na kulipiza
kisasi damu yetu?” 11 Kisha kila mmoja alipewa kanzu nyeupe na wakaambiwa
kuwa wanapaswa kusubiri kidogo hata itakapotimia hesabu kamili ya watumishi
wenzao na ndugu zao wa kike na wa kiume itakapotimia ambao watauawa, kama
vile ambavyo wao waliuawa. 12 Wakati mwanakondoo alipofungua muhuri ya sita,
nilitazama na palikuwa na tetemeko kuu. Jua likawa jeusi kama gunia la singa,
na mwezi mzima ukawa kama damu. 13 Nyota za mbinguni zikaanguka katika
nchi, kama mtini upukutishavyo matunda yake ya wakati wa baridi unapotikiswa
na kimbunga. 14 Anga ilitoweka kama gombo lililoviringishwa. Kila mlima na
kisiwa vilihamishwa mahali pake. 15 Kisha wafalme wa nchi na watu maarufu
na majemadari, matajiri, wenye nguvu, na kila mmoja aliye mtumwa na huru,
wakajificha katika mapango na katika miamba ya milima. 16 Wakaiambia milima
na miamba, “Tuangukieni! Tuficheni dhidi ya uso wake aketiye kwenye kiti cha enzi
na kutoka hasira ya mwanakondoo. 17 Kwa kuwa siku kuu ya gadhabu yao imewadia,
na ni nani awezaye kusimama?”

# 7

1 Baada ya haya niliona malaika wanne wamesimama kwenye kona nne za dunia,
wamezuia pepo nne za nchi kwa nguvu ili kwamba pasiwe na upepo unaovuma
katika nchi, juu ya bahari au dhidi ya mti wowote. 2 Nikaona malaika mwingine
akija kutoka mashariki, aliyekuwa na muhuri wa Mungu aliye hai. Akalia kwa
sauti kuu kwa malaika wanne ambao walipewa ruhusa ya kudhuru nchi na bahari:
3 “Msiidhuru nchi, bahari, au miti mpaka tutakapokuwa tumekwishaweka muhuri
katika paji za vichwa vya watumishi wa Mungu wetu.” 4 Nikasikia idadi ya wale
waliotiwa muhuri: 144, 000, ambao walitiwa muhuri kutoka kila kabila ya watu wa
Israel: 5 12, 000 kutoka katika kabila ya Yuda walitiwa muhuri, 12, 000 kutoka katika
kabila ya Rubeni, 12, 000 kutoka katika kabila ya Gadi. 6 12, 000 kutoka katika kabila
ya Asheri, 12, 000 kutoka katika kabila ya Naftali, 12, 000 kutoka katika kabila ya
Manase. 7 12, 000 kutoka kabila ya Simioni, 12, 000 kutoka kabila ya Lawi, 12, 000
kutoka kabila ya Isakari, 8 12, 000 kutoka kabila ya Zebuloni, 12, 000 kutoka kabila ya

Yusufu, na 12, 000 kutoka kabila ya Benyamini walitiwa muhuri. [9] Baada ya mambo
haya nilitazama, na kulikuwa na umati mkubwa ambao hapana mtu angeweza
kuuhesabu - kutoka kila taifa, kabila, jamaa, na lugha - wamesimama mbele ya
kiti cha enzi na mbele ya Mwanakondoo. Walikuwa wamevaa kanzu nyeupe na
wana matawi ya mitende mikononi mwao, [10] na walikuwa wakiita kwa sauti ya juu:
"Wokovu ni kwa Mungu ambaye ameketi katika kiti cha enzi, na kwa Mwanakondoo!"
[11] Malaika wote waliokuwa wamesimama kuzunguka kiti cha enzi na kuwazunguka
wale wazee pamoja na wenye uhai wanne, wakainama chini ardhini na wakaweka
nyuso zao juu ya ardhi mbele ya kiti cha enzi na wakamwabudu Mungu, [12] wakisema,
"Amina! Sifa, utukufu, hekima, shukurani, heshima, uwezo na nguvu viwe kwa
Mungu wetu milele na milele! Amina!" [13] Kisha mmoja wa wale wazee akaniuliza,
"hawa ni akina nani waliovaa kanzu nyeupe, na wametoka wapi? [14] Nikamwambia,
"Bwana mkubwa, unajua wewe," na akaniambia, "Hawa ni wale waliotoka katika
dhiki kuu. Wamezifua kanzu zao na kuzifanya nyeupe kwa damu ya Mwanakondoo.
[15] Kwa sababu hii, wako mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, na wanamwabudu yeye
usiku na mchana katika hekalu lake. Yeye aliye keti juu ya kiti cha enzi atasambaza
hema yake juu yao. [16] Hawataona njaa tena, wala kiu tena. Jua halitawachoma, wala
joto la kuunguza. [17] Kwa kuwa Mwanakondoo aliye katikati ya kiti cha enzi atakuwa
mchungaji wao, na atawaongoza katika chemchemi ya maji ya uzima, na Mungu
atafuta kila chozi katika macho yao."

# 8

[1] Wakati Mwanakondoo alipofungua muhuri ya saba, kukawa na ukimya mbinguni
takribani nusu saa. [2] Kisha nikaona malaika saba wasimamao mbele za Mungu,
na wakapewa tarumbeta saba. [3] Malaika mwingine akaja, ameshikilia bakuli ya
dhahabu yenye uvumba, amesimama madhabahuni. Akapewa uvumba mwingi ili
kwamba autoe pamoja na maombi ya waamini wote katika madhabahu ya dhahabu
mbele ya kiti cha enzi. [4] Moshi wa ule uvumba, pamoja na maombi ya waamini,
ukapanda juu mbele za Mungu kutoka mkononi mwa malaika. [5] Malaika akatwaa
bakuli la uvumba na akalijaza moto kutoka kwenye madhabahu. Kisha akalitupa
chini juu ya nchi, na kukatokea sauti za radi, miale ya radi na tetemeko la nchi.
[6] Wale malaika saba ambao walikuwa na tarumbeta saba wakawa tayari kuzipiga.
[7] Malaika wa kwanza akaipiga tarumbeta yake, na kukatokea mvua ya mawe na
moto uliochanganyikana na damu. Vikatupwa chini katika nchi ili kwamba theluthi
yake iungue, theluthi ya miti ikaungua na nyasi zote za kijani zikaungua. [8] Malaika
wa pili akaipiga tarumbeta yake, na kitu kama mlima mkubwa uliokuwa unaungua
kwa moto ukatupwa baharini. Theluthi ya bahari ikawa damu, [9] theluthi ya viumbe
hai katika bahari vikafa, na theluthi ya meli zikaharibiwa. [10] Malaika wa tatu
akaipiga tarumbeta yake, na nyota kubwa ikaanguka kutoka mbinguni, ikimulika
kama kurunzi, juu ya theluthi ya mito na chemichemi za maji. [11] Jina la nyota ni
pakanga. Theluthi ya maji ikawa pakanga, na watu wengi wakafa kutokana na maji
yaliyokuwa machungu. [12] Malaika wa nne alipiga tarumbeta yake, na theluthi ya
jua ikapigwa, pamoja na theluthi ya mwezi na theluthi ya nyota. Kwa hiyo theluthi
ya vyote ikageuka kuwa giza; theluthi ya mchana na theluthi ya usiku havikuwa na
mwanga. [13] Nilitazama, na nikasikia tai aliye kuwa anaruka katikati ya anga, akiita
kwa sauti kuu, "Ole, ole, ole, kwa wale wakaao katika nchi, kwa sababu ya mlipuko
wa tarumbeta iliyosalia ambayo imekaribia kupigwa na malaika watatu."

# 9

[1] Kisha malaika wa tano alipiga tarumbeta yake. Niliona nyota kutoka mbinguni

iliyokuwa imeanguka kwenye dunia. Nyota ilipewa ufunguo wa shimo linaloelekea
kwenye shimo lisilo na mwisho. 2 Alifungua shimo lisilo na kikomo, na moshi
ukapanda juu kwa safu kutoka ndani ya shimo kama moshi kutoka katika tanuru
kubwa. Jua na anga vilibadilika vikawa giza kwa sababu ya moshi uliotoka shimoni.
3 Ndani ya moshi nzige walitoka kuja juu ya dunia, nao walipewa nguvu kama ile ya
nge juu ya dunia. 4 Waliambiwa kutokudhuru majani katika nchi au mmea wowote
wa kijani au mti, isipokuwa tu watu ambao hawakuwa na muhuri wa Mungu katika
paji za nyuso zao. 5 Hawakupewa ruhusa ya kuwaua hao watu, bali kuwatesa tu kwa
miezi mitano. Uchungu wao ulikuwa kama ule wa kuumwa na nge amwumapo mtu.
6 Katika siku hizo watu watatafuta kifo, lakini hawatakipata. Watatamani kufa, lakini
kifo kitawakimbia. 7 Nzige walifanana na farasi walioandaliwa kwa vita. Kwenye
vichwa vyao kulikuwa na kitu kama taji ya dhahabu na nyuso zao zilikuwa kama za
binadamu. 8 Walikuwa na nywele kama za wanawake na meno yao yalikuwa kama ya
simba. 9 Walikuwa na vifua kama vifua vya chuma na sauti ya mabawa yao ilikuwa
kama sauti ya magari mengi ya vita na farasi wakimbiao kwenda vitani. 10 Walikuwa
na mikia inayouma kama nge; katika mikia yao walikuwa na nguvu ya kudhuru
watu kwa miezi mitano. 11 Walikuwa naye kama mfalme juu yao malaika wa shimo
lisilokuwa na mwisho. Jina lake katika Kiebrania ni Abadoni, na katika Kiyunani
ana jina Apolioni. 12 Ole ya kwanza imepita. Angalia! Baada ya hili kuna maafa
mawili yaja. 13 Malaika wa sita alipiga tarumbeta yake, na nikasikia sauti ikitoka
katika pembe ya madhabahu ya dhahabu ambayo iko mbele za Mungu. 14 Sauti
ilimwambia malaika wa sita aliyekuwa na tarumbeta, “Waachie malaika wanne
ambao wamefungwa katika mto mkubwa Efrata.” 15 Malaika wale wanne waliokuwa
wameandaliwa kwa saa hiyo maalumu, siku hiyo, mwezi huo, na mwaka huo,
waliachiwa wawaue theluthi ya wanadamu. 16 Idadi ya maaskari waliokuwa juu ya
farasi ilikuwa 200, 000, 000. Nilisikia idadi yao. 17 Hivi ndivyo nilivyoona farasi katika
maono yangu na wale waliopanda juu yao: Vifua vyao vilikuwa vyekundu kama
moto, bluu iliyoiva na njano isiyoiva. Vichwa vya farasi vilifanana na vichwa vya
simba, na midomoni mwao ulitoka moto, moshi na salfa. 18 Theluthi ya wanadamu
waliuawa na haya mapigo matatu: moto, moshi, na salfa iliyotoka katika midomo
yao. 19 Kwa kuwa nguvu ya farasi ilikuwa katika midomo yao na katika mikia
yao—kwa kuwa mikia yao ilikuwa kama nyoka, na walikuwa na vichwa ambavyo
walitumia kuwatia majeraha wanadamu. 20 Watu waliobaki, wale ambao walikuwa
hawajauawa na mapigo haya, hawakutubia matendo yao waliyokuwa wamefanya,
wala hawakuacha kuabudu mapepo na miungu ya dhahabu, fedha, shaba, mawe
na miti—vitu ambavyo haviwezi kuona, kusikia au kutembea. 21 Wala hawakutubia
uuaji wao, uchawi wao, uasherati wao au njia zao za wizi.

# 10

1 Kisha nikaona malaika mwingine mkuu akishuka chini kutoka mbinguni. Alikuwa
amefungwa katika wingu, na kulikuwa na upinde wa mvua juu ya kichwa chake. Uso
wake ulikuwa kama jua na miguu yake ilikuwa kama nguzo za moto. 2 Alishikilia
gombo dogo katika mkono wake lililokuwa limefunuliwa, naye aliweka mguu wake
wa kulia juu ya bahari na mguu wake wa kushoto juu ya nchi kavu. 3 Kisha
alipaza sauti ya juu kama simba aungurumapo, na wakati alipopaza sauti radi saba
ziliunguruma. 4 Wakati radi saba zilipounguruma, nilikuwa nakaribia kuandika,
lakini nilisikia sauti kutoka mbinguni ikisema, “Tunza iwe siri kile ambacho radi saba
zimesema. Usiiandike.” 5 Kisha malaika niliyemwona amesimama juu ya bahari na
nchi kavu, aliinua mkono wake juu mbinguni 6 na kuapa kwa yule aishiye milele
na milele —aliyeumba mbingu na vyote vilivyomo, dunia na vyote vilivyomo, na

bahari na vyote vilivyomo: “Hakutakuwepo kuchelewa tena. 7 Lakini katika siku
ile, wakati malaika wa saba atakapokaribia kupiga tarumbeta yake, ndipo siri ya
Mungu itakuwa imetimizwa, kama alivyotangaza kwa watumishi wake manabii.”
8 Sauti niliyosikia kutoka mbinguni iliniambia tena: “Nenda, chukua gombo dogo
lililofunuliwa ambalo kiko katika mkono wa malaika aliyesimama juu ya bahari na
juu ya nchi kavu.” 9 Kisha nilikwenda kwa malaika na kumwambia anipe gombo
dogo. Aliniambia, “Chukua gombo na ule. Litalifanya tumbo lako liwe na uchungu,
lakini katika mdomo wako litakuwa tamu kama asali.” 10 Nilichukua gombo dogo
kutoka mkononi mwa malaika na kulila. Lilikuwa kitamu kama asali katika mdomo
wangu, lakini baada ya kula, tumbo langu lilikuwa na uchungu. 11 Kisha baadhi ya
sauti ziliniambia, “Unapaswa kutabiri tena kuhusu watu wengi, mataifa, lugha, na
wafalme.”

# 11

1 Nilipewa mwanzi wa kutumia kama fimbo ya kupimia. Niliambiwa, “Ondoka
na ukapime hekalu la Mungu na madhabahu, na wale wanaoabudu ndani yake.
2 Lakini usipime eneo la ua wa nje ya hekalu, kwa kuwa wamepewa watu wa
Mataifa. Wataukanyaga mji mtakatifu kwa muda wa miezi arobaini na miwili.
3 Nitawapa mashahidi wangu wawili mamlaka ya kutabiri kwa muda wa siku 1,
260, wakiwa wamevaa magunia.” 4 Hawa mashahidi ni miti miwili ya mizeituni na
vinara viwili ambavyo vimesimama mbele ya Bwana wa dunia. 5 Kama mtu yeyote
ataamua kuwadhuru, moto hutoka vinywani mwao na kuwadhuru adui zao. Yeyote
anayetaka kuwadhuru lazima auawe kwa njia hii. 6 Hawa mashahidi wana uwezo
wa kufunga anga ili kwamba mvua isinyeshe wakati wanatabiri. Wana nguvu ya
kubadili maji kuwa damu na kuipiga nchi kwa kila aina ya pigo wakati wowote
wakitaka. 7 Wakati watakapokuwa wamemaliza ushuhuda wao, yule mnyama
anayetoka kwenye shimo lisilo na mwisho atafanya vita dhidi yao. Atawashinda
na kuwaua. 8 Miili yao italala katika mtaa wa mji mkuu (ambao kimfano unaitwa
Sodoma na Misri) ambapo Bwana wao alisulubiwa. 9 Kwa siku tatu na nusu baadhi
kutoka katika jamaa za watu, kabila, lugha na kila taifa watatazama miili yao na
hawatatoa kibali kuwekwa katika kaburi. 10 Wale wanaoishi katika nchi watafurahi
kwa ajili yao na kushangilia, hata kutumiana zawadi kwa sababu hao manabii wawili
waliwatesa wale walioishi katika nchi. 11 Lakini baada ya siku tatu na nusu pumzi
ya uhai kutoka kwa Mungu itawaingia nao watasimama kwa miguu yao. Hofu kuu
itawaangukia wale wanaowaona. 12 Kisha watasikia sauti kuu kutoka mbinguni
ikiwaambia, “Njoni huku!” Nao watakwenda juu mbinguni katika wingu, wakati
adui zao wakitazama. 13 Katika saa hiyo kutakuwepo na tetemeko kuu la ardhi
na moja ya kumi ya mji itaanguka. Watu elfu saba watauawa katika tetemeko na
watakaobaki hai wataogopeshwa na kumpa utukufu Mungu wa mbinguni. 14 Ole ya
pili imepita. Angalia! Ole ya tatu inakuja upesi. 15 Kisha malaika wa saba alipiga
tarumbeta yake, na sauti kubwa zilinena mbinguni na kusema, “Ufalme wa dunia
umeshakuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake. Atatawala milele na milele.”
16 Kisha wazee ishirini na wanne waliokuwa wameketi kwenye viti vya enzi mbele
ya Mungu walianguka wenyewe chini kwenye ardhi, nyuso zao zimeinama chini, nao
walimwabudu Mungu. 17 Walisema, “Twatoa shukrani zetu kwako, Bwana Mungu,
mtawala juu ya vyote, ambaye upo na ambaye ulikuwepo, kwa sababu umetwaa
nguvu yako kuu na kuanza kutawala. 18 Mataifa walikasirika, lakini gadhabu yako
imekuja. Wakati umefika kwa wafu kuhukumiwa na wewe kuwazawadia watumishi
wako manabii, waamini na wale walio na hofu ya jina lako, wote wawili wasiofaa kitu
na wenye nguvu. Na wakati wako umefika wa kuwaharibu wale ambao wamekuwa
wakiiharibu dunia.” 19 Kisha hekalu la Mungu mbinguni lilifunuliwa na sanduku la

agano lake lilionekana ndani ya hekalu lake. Kulikuwa na miali ya mwanga, kelele, ngurumo za radi, tetemeko la ardhi na mawe ya mvua.

# 12

1 Ishara kuu ilionekana mbinguni: mwanamke aliyefunikwa na jua, na akiwa
na mwezi chini ya miguu yake; na taji ya nyota kumi na mbili ilikuwa juu ya
kichwa chake. 2 Alikuwa na mimba na alikuwa analia kwa ajili ya maumivu ya
kuzaa—katika uchungu wa kujifungua. 3 Na ishara nyingine ilionekana mbinguni:
Tazama! Kulikuwa na joka mwekundu mkubwa ambaye alikuwa na vichwa saba
na pembe kumi, na kulikuwa na taji saba kwenye vichwa vyake. 4 Mkia wake
ulikokota theluthi moja ya nyota mbinguni na kuzitupa chini duniani. Joka alisimama
mbele ya mwanamke aliyekuwa anakaribia kuzaa, ili kwamba wakati anazaa, apate
kummeza mtoto wake. 5 Alimzaa mwana, mtoto wa kiume, ambaye atayatawala
mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Mtoto wake alinyakuliwa juu kwa Mungu na
kwenye kiti chake cha enzi, 6 na mwanamke alikimbilia nyikani, mahali ambapo
Mungu alikuwa ameandaa eneo kwa ajili yake, ili aweze kuhudumiwa kwa siku 1,
260. 7 Sasa kulikuwa na vita mbinguni. Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule
joka; naye joka mkubwa na malaika zake wakapigana nao. 8 Lakini joka hakuwa
na nguvu za kutosha kushinda. Kwa hiyo haikuwepo tena nafasi mbinguni kwa ajili
yake na malaika zake. 9 Joka mkubwa—yule nyoka wa zamani aitwaye ibilisi au
Shetani ambaye hudanganya - dunia nzima akatupwa chini katika dunia, na malaika
zake wakatupwa chini pamoja naye. 10 Kisha nikasikia sauti kubwa kutoka mbinguni:
“Sasa wokovu umekuja, nguvu—na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo
wake. Kwa kuwa mshitaki wa ndugu zetu ametupwa chini—ambaye aliwashitaki
mbele za Mungu wetu mchana na usiku. 11 Walimshinda kwa damu ya Mwanakondoo
na kwa neno la ushuhuda wao, kwa maana hawakupenda sana maisha yao, hata kufa.
12 Kwa hiyo, shangilieni, ninyi mbingu, na wote mnaokaa ndani yake. Lakini ole wa
nchi na bahari kwa sababu mwovu ameshuka kwenu. Amejawa na hasira kali, kwa
sababu anajua kwamba ana muda mchache tu. 13 Wakati joka alipotambua kuwa
ametupwa chini kwenye nchi, alimfuata mwanamke ambaye alikuwa amezaa mtoto
wa kiume. 14 Lakini mwanamke alipewa mabawa mawili ya tai mkubwa, ili kwamba
aweze kuruka hadi kwenye eneo lililoandaliwa kwa ajili yake kule jangwani, eneo
ambalo angeweza kutunzwa, kwa wakati, nyakati na nusu wakati-mahali asipoweza
kupafikia huyo nyoka. 15 Nyoka alimwaga maji kutoka mdomoni mwake kama mto,
ili afanye gharika ya kumgharikisha. 16 Lakini ardhi ilimsaidia mwanamke. Ilifunua
kinywa chake na kuumeza mto alioutema joka kutoka kinywani mwake. 17 Kisha
joka akamkasirikia mwanamke naye aliondoka na kufanya vita na uzao wake wote—
wale wanaotii amri za Mungu na kushikilia ushuhuda kuhusu Yesu. 18 Kisha joka
alisimama juu ya mchanga ufukwe wa bahari.

# 13

1 Kisha nikaona mnyama akitoka kwenye bahari. Alikuwa na pembe kumi na
vichwa saba. Katika pembe zake kulikuwa na taji kumi, na katika kichwa chake
kulikuwa na maneno ya kufuru kwa Mungu. 2 Huyu mnyama niliyemuona ni kama
chui. Miguu yake ilikuwa kama ya dubu, na mdomo wake ulikuwa kama wa simba.
Yule joka akampa nguvu, na katika kiti chake cha enzi, na mamlaka yenye nguvu
sana ya kutawala. 3 Kichwa cha mnyama mmojawapo kilionekana kuwa na jeraha
kubwa ambalo lingesababisha mauti yake. Lakini jeraha lake likapona, na dunia
yote ikashangazwa na ikamfuata mnyama. 4 Pia wakamwabudu joka, maana alimpa
mamlaka yule mnyama. Wakamwabudu mnyama pia, na wakaendelea kusema,

“Nani kama mnyama? na “Nani atapigana naye?” [5] Mnyama akapewa mdomo ili
azungumze maneno ya kujisifu na matusi. Aliruhusiwa kuwa na mamlaka kwa
miezi arobaini na miwili. [6] Hivyo mnyama alifungua mdomo wake kuongea matusi
dhidi ya Mungu, akalitukana jina lake, eneo alililokuwa akiishi na wale wanaoishi
mbinguni. [7] Mnyama aliruhusiwa kufanya vita na waamini na kuwashinda. Pia,
alipewa mamlaka juu ya kila kabila, watu, lugha na taifa. [8] Wote walioishi duniani
watamwabudu yeye, kila mmoja ambaye jina lake halijaandikwa, toka uumbaji wa
dunia, katika kitabu cha uzima, ambacho ni cha Mwana Kondoo, ambaye alichinjwa.
[9] Ikiwa yeyote ana sikio, na asikilize. [10] Ikiwa mmojawapo amechukuliwa mateka,
na kwenye mateka ataenda. Ikiwa mmojawapo ataua kwa upanga, kwa upanga
atauawa. Huu ni mwito wa utulivu na uvumilivu na imani kwa hao walio watakatifu.
[11] Tena nikaona mnyama mwingine anakuja kutoka katika nchi. Alikuwa mwenye
pembe mbili kama kondoo na akazungumza kama joka. [12] Alionyesha mamlaka yote
katika mnyama yule wa kwanza katika uwepo wake, na kufanya katika dunia na
wale walioishi wakimuabudu yule mnyama wa kwanza, yule ambaye jeraha lake
limepona. [13] Akafanya miujiza yenye nguvu, hata akafanya moto ushuke katika
dunia kutoka mbinguni mbele ya watu, [14] na kwa ishara aliruhusiwa kufanya,
akawadanganya hao wakaao katika dunia, akiwaambia kutengeneza sanamu kwa
heshima ya mnyama ambaye alikuwa amejeruhiwa kwa upanga, lakini bado aliishi.
[15] Aliruhusiwa kutoa pumzi katika ile sanamu ya mnyama ili sanamu iweze kusema
na kusababisha wale wote waliokataa kumwabudu mnyama wauawe. [16] Pia
akalazimisha kila mmoja, asiye na thamani na mwenye nguvu, tajiri na maskini,
huru na mtumwa, kupokea alama katika mkono wa kuume au katika paji la uso.
[17] Ilikuwa haiwezekani kwa kila mtu kuuza au kununua isipokuwa mwenye alama
ya mnyama, na hii ni namba yenye kuwakilisha jina lake. [18] Hii inahitaji busara.
Ikiwa yeyote ana ufahamu, mwache aweze kufanya hesabu ya namba ya mnyama.
Maana ni namba ya kibinadamu. Namba yake ni 666.

# 14

[1] Nilitazama na nikaona Mwana Kondoo amesimama mbele yangu juu ya Mlima
Sayuni. Pamoja naye walikuwa 144, 000 wenye jina lake na jina la Baba yake
limeandikwa katika vipaji vya nyuso zao. [2] Nikasikia sauti kutoka mbinguni ikisikika
kama ngurumo za maji mengi na sauti kubwa ya radi. Sauti niliyoisikia ni kama
wapiga vinubi wapigao vinubi vyao. [3] Wakiimba wimbo mpya mbele za kiti cha
enzi na mbele za wenye uhai wanne na wazee. Hakuna hata mwenye uwezo
wa kujifunza huo wimbo isipokuwa kwa 144, 000 ambao wamekombolewa kutoka
duniani. [4] Hawa ni wale ambao hawakujichafua wenyewe kwa wanawake, maana
walijitunza wenyewe dhidi ya matendo ya zinaa. Ni hawa ambao walimfuata
Mwana Kondoo popote alipoenda. Hawa walikombolewa kutoka kwa wanadamu
wakiwa matunda ya kwanza kwa Mungu na kwa Mwana Kondoo. [5] Hakuna uongo
uliopatikana katika vinywa vyao; hawalaumiwi. [6] Nikaona malaika mwingine
akiruka katikati ya mbingu, ambaye mwenye ujumbe wa mbinguni wa habari njema
kwa kuwatangazia wenye kuishi duniani kwa kila taifa, kabila, lugha, na watu.
[7] Akawaita kwa sauti kuu, “Mwogopeni Mungu na mpeni utukufu. Kwa maana muda
wa hukumu umekaribia. Mwabuduni yeye, yeye aliyeumba mbingu, na dunia, na
bahari, na chemchemi za maji.” [8] Malaika mwingine - malaika wa pili - akafuata
akisema, “Umeanguka, umeanguka Babeli mkuu, ambaye uliwanywesha mataifa
divai ya ukahaba, divai ambayo ilileta ghadhabu juu yake.” [9] Malaika mwingine
- malaika wa tatu - aliwafuata, akasema kwa sauti kuu, “Yeyote atakayemwabudu
huyo mnyama na sanamu yake, na kupokea alama katika paji lake la uso au mkononi,

[10] yeye pia atakunywa divai ya ghadhabu ya Mungu, divai ambayo imeandaliwa na
kumwagwa bila kuchanganywa katika kikombe cha hasira yake. Mtu atakayekunywa
atateswa kwa moto na moto wa kiberiti mbele za malaika zake watakatifu na mbele
za Mwana Kondoo. [11] Na moshi wa maumivu yao ukaenda milele na milele, na
hawakuwa na mapumziko mchana au usiku - hao waabuduo mnyama na sanamu
yake, na kila mtu aliyepokea alama ya jina lake. [12] Huu ni wito wa subira na
uvumilivu kwa waamini, wale ambao hutii amri za Mungu na imani katika Yesu."
[13] Nilisikia sauti kutoka mbinguni ikisema, "Andika haya: Heri wafu wafao katika
Bwana." "Ndiyo," asema Roho, "ili waweze kupumzika kutoka kwenye kazi zao,
maana matendo yao yatawafuata." [14] Nilitazama na nikaona kulikuwa na wingu
jeupe, na aliyeketi kwenye wingu ni mmoja aliyekuwa na mfano wa Mwana wa Mtu.
Alikuwa na taji ya dhahabu katika kichwa chake na mundu mkali katika mkono
wake. [15] Malaika mwingine tena alikuja kutoka kwenye hekalu na aliita kwa sauti kuu
kwenda kwa yule aliyekaa katika wingu: "Chukua mundu wako na uanze kuvuna.
Kwa kuwa muda wa mavuno umeshawadia, maana mavuno yaliyo katika dunia
yameshaiva." [16] Tena yule aliyekuwa kwenye wingu aliupitisha mundu wake juu ya
dunia, na dunia ikavunwa. [17] Na malaika mwingine akaja kutoka kwenye hekalu la
mbinguni; naye alikuwa na mundu mkali. [18] Na bado malaika mwingine akaja kutoka
kwenye madhabahu, na malaika aliyekuwa na mamlaka juu ya moto. Akamwita
kwa sauti kuu malaika ambaye alikuwa na mundu mkali, "Chukua mundu mkali na
uyakusanye matawi ya mzabibu kutoka kwenye mzabibu wa nchi, kwa kuwa zabibu
sasa zimeiva." [19] Malaika alipeleka mundu wake katika dunia na alikusanya mavuno
ya zabibu ya dunia na alirusha katika pipa kubwa la divai ya ghadhabu ya Mungu.
[20] Chujio la divai lilipondwapondwa nje ya mji na damu ikamwagika kutoka katika
hicho kimo cha hatamu ya farasi, kwa stadia 1, 600.

# 15

[1] Tena nikaona ishara nyingine mbinguni, kubwa na yenye kushangaza; Kulikuwa
na malaika saba wenye mapigo saba, ambayo yalikuwa mapigo ya mwisho (katika
hayo hasira ya Mungu ilikuwa imetimilika). [2] Niliona kile kilichotokea kuwa bahari
ya bilauri iliyochanganywa na moto, na ikasimama pembeni mwa bahari ambapo
wale waliokuwa washindi dhidi ya mnyama na sanamu yake, na juu ya namba
inayowakilisha jina lake. Walikuwa wameshikilia vinubi walivyopewa na Mungu.
[3] Walikuwa wakiimba wimbo wa Musa, mtumishi wa Mungu, na wimbo wa Mwana
Kondoo: "Kazi zako ni kubwa na zenye kushangaza, Bwana Mungu, utawalaye
vyote. Mwaminifu na njia zako ni za kweli, Mfalme wa mataifa. [4] Nani atashindwa
kukuhofu wewe Bwana na kulitukuza jina lako? Kwa kuwa wewe peke yako ni
mtakatifu. Mataifa yote yatakuja na kukuabudu mbele zako kwa sababu u mwema
na matendo yako yamejulikana." [5] Baada ya mambo hayo nilitazama, na sehemu
takatifu sana, ambapo palikuwa na hema ya ushuhuda, iliyofungukia mbinguni.
[6] Kutoka mahali patakatifu sana wakaja malaika saba wenye mapigo saba, wamevaa
mavazi safi, kitani yenye kung'aa na mshipi wa dhahabu kuzunguka vifua vyao.
[7] Mmoja wa wale wenye uhai wanne akatoa kwa malaika saba mabakuli saba ya
dhahabu yaliyojaa ghadhabu ya Mungu mwenye kuishi milele na milele. [8] Mahali
patakatifu sana kulijawa moshi kutoka kwenye utukufu wa Mungu na kutoka kwenye
uwezo wake. Hakuna hata mmoja aliyeweza kuingia mpaka mapigo saba ya malaika
saba yalipokamilika.

# 16

[1] Nikasikia sauti kubwa ikiita kutoka kwenye sehemu ya patakatifu na ikasema kwa

wale malaika saba, "Nenda na ukamwage juu ya dunia mabakuli saba ya ghadhabu
ya Mungu." 2 Malaika wa kwanza aliend a na kumwaga bakuli lake katika dunia;
majeraha mabaya na yenye maumivu makali yalikuja kwa watu wenye alama ya
mnyama, kwa wale ambao waliabudu sanamu yake. 3 Malaika wa pili alimwaga
bakuli lake katika bahari; ikawa kama damu ya mtu aliyekufa, na kila kiumbe hai
katika bahari kilikufa. 4 Malaika wa tatu akamwaga bakuli lake katika mito na
katika chemichemi za maji; zikawa damu. 5 Nikasikia malaika wa maji akisema,
"Wewe ni mwaminifu - mmoja uliyepo na uliyekuwako, Mtakatifu - kwa sababu
umezileta hukumu hizi. 6 Kwa sababu walimwaga damu za waamini na manabii,
umewapa wao kunywa damu; ndicho wanachostahili." 7 Nikasikia madhabahu
ikijibu, "Ndiyo! Bwana Mungu mwenye kutawala juu ya vyote, hukumu zako ni
kweli na za haki." 8 Malaika wa nne akamwaga kutoka kwenye bakuli lake juu
ya jua, na likapewa ruhusa kuunguza watu kwa moto. 9 Waliunguzwa kwa joto
lenye kutisha, na wakalikufuru neno la Mungu, mwenye nguvu juu ya mapigo yote.
Hawakutubu wala kumpa yeye utukufu. 10 Malaika wa tano akamwaga kutoka
kwenye bakuli lake katika kiti cha enzi cha mnyama, na giza likaufunika ufalme
wake. Walisaga meno katika maumivu makali. 11 Wakamtukana Mungu wa mbinguni
kwa sababu ya maumivu yao na majeraha yao, na bado waliendelea kutokutubu
kwa kile walichotenda. 12 Malaika wa sita alimwaga kutoka kwenye bakuli lake
katika mto mkubwa, Frati, na maji yake yakakauka ili kuweza kuandaa njia kwa
wafalme watakaokuja kutoka mashariki. 13 Nikaona roho tatu chafu zilizoonekana
kama chura watokao nje ya mdomo wa yule joka, yule mnyama, na yule nabii wa
uongo. 14 Ni roho za pepo zitendazo ishara na miujiza. Walikuwa wakienda kwa
wafalme wa dunia yote ili kuweza kuwakusanya pamoja kwa vita katika siku kuu ya
Mungu, mwenye kutawala juu ya vyote. 15 ("Tazama! Ninakuja kama mwizi! Heri
yule adumuye katika kukesha, atunzaye mavazi yake ili asiweze kwenda nje uchi na
kuiona aibu yake.") 16 Waliwaleta pamoja katika sehemu iliyoitwa katika kiebrania
Amagedoni. 17 Malaika wa saba alimwaga kutoka kwenye bakuli lake katika anga.
Kisha sauti kuu ikasikika kutoka pakatifu na kutoka kwenye kiti cha enzi, ikisema,
"Imekwisha!" 18 Kulikuwa na miale ya mwanga wa radi, ngurumo, vishindo vya radi,
na tetemeko la kutisha - tetemeko kubwa la ardhi ambalo halijawahi kutokea duniani
tangu wanadamu wamekuwepo duniani, hivyo ni tetemeko kubwa zaidi. 19 Mji
mkuu uligawanyika katika sehemu tatu, na miji ya mataifa ikaanguka. Kisha Mungu
akamkumbusha Babeli mkuu, na akaupa mji huo kikombe kilichokuwa kimejaa
divai kutoka kwenye ghadhabu yake iliyo kali. 20 Kila kisiwa kikapotea na milima
haikuonekana tena. 21 Mvua kubwa ya mawe, ikiwa na uzito wa talanta, ikashuka
kutoka mbinguni juu ya watu, na wakamlaani Mungu kwa mapigo ya mvua ya mawe
kwa sababu lile pigo lilikuwa baya sana.

# 17

1 Mmoja wa malaika saba aliyekuwa na vitasa saba alikuja na kuniambia, "Njoo,
nitakuonesha hukumu ya kahaba mkuu akaaye juu ya maji mengi, 2 ambaye wafalme
wa nchi wamefanya mambo ya uzinzi naye na juu ya mvinyo wa uzinzi wake wakaao
duniani wameleweshwa." 3 Malaika akanichukua katika Roho mpaka nyikani,
na nilimwona mwanamke amekaa juu ya mnyama mwekundu aliyejaa majina ya
matukano. Mnyama alikuwa na vichwa saba na pembe kumi. 4 Mwanamke alivikwa
nguo ya zambarau na nyekundu na amepambwa kwa dhahabu, mawe ya thamani,
na lulu. Alikuwa ameshikilia mkononi mwake kikombe cha dhahabu kilichojaa vitu
vya machukizo ya uchafu wa uasherati wake. 5 Juu ya paji la uso wake limeandikwa
jina la siri: "BABELI MKUU, MAMA WA MAKAHABA NA YA VITU VYA MACHUKIZO YA

NCHI.” 6 Nikaona ya kuwa mwanamke huyo alikuwa amelewa kwa damu ya waumini
na damu ya waliokufa kwa ajili ya Yesu. Wakati nilipomwona, nilikuwa na mshangao
mkuu. 7 Lakini malaika akaniambia, “Kwa nini unashangaa? Nitakueleza maana ya
mwanamke na mnyama amchukuaye (mnyama huyo mwenye vichwa saba na zile
pembe kumi). 8 Mnyama uliyemwona alikuwepo, hayupo tena sasa, lakini yuko tayari
kupanda kutoka katika shimo lisilo na mwisho. Kisha ataendelea na uharibifu. Wale
wakaao juu ya nchi, wale ambao majina yao hayakuandikwa kwenye kitabu cha
uzima tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu - watashangaa wamwonapo mnyama
aliyekuwepo, kwamba hayupo sasa, lakini yupo karibu kuja. 9 Wito huu ni kwa ajili
ya akili zilizo na hekima. Vichwa saba ni milima saba ambapo mwanamke alikaa juu
yake. 10 Nayo pia ni wafalme saba. Wafalme watano wameanguka, mmoja yupo, na
mwingine hajaja bado; wakati atakapokuja, atakaa kwa muda mfupi tu. 11 Mnyama
aliyekuwepo, lakini sasa hayupo, yeye pia ni mfalme wa nane; lakini ni mmoja wa
wale wafalme saba, na anaenda kwenye uharibifu. 12 Zile pembe kumi ulizoziona
ni wafalme kumi ambao hawajapokea ufalme, lakini watapokea mamlaka kama
wafalme kwa saa moja pamoja na mnyama. 13 Hawa wana shauri moja, na watampa
nguvu zao na mamlaka yule mnyama. 14 Watafanya vita baina yao na Mwana
kondoo. Lakini Mwana kondoo atawashinda kwa sababu ni Bwana wa mabwana na
Mfalme wa wafalme - na katika yeye tuliitwa, tulichaguliwa, waaminifu.” 15 Malaika
akaniambia, “Yale maji uliyoyaona, hapo alipoketi yule kahaba ni watu, makutano,
mataifa na lugha. 16 Zile pembe kumi ulizoziona - hizo na yule mnyama watamchukia
yule kahaba. Nao watamfanya kuwa mpweke na uchi, watamla mwili wake, na
watauteketeza kwa moto. 17 Maana Mungu ameweka mioyoni mwao kubeba kusudi
lake kwa makubaliano ya kumpa mnyama nguvu zao kumtawala mpaka maneno ya
Mungu yatakapotimia. 18 Yule mwanamke uliyemwona ni mji ule mkubwa utawalao
juu ya wafalme wa nchi.”

# 18

1 Baada ya vitu hivi nilimwona malaika mwingine akishuka chini kutoka mbinguni.
Yeye alikuwa na mamlaka kuu, na nchi iliangazwa kwa utukufu wake. 2 Alilia
kwa sauti kuu, akisema, “Umeanguka, umeanguka, ule mji mkuu Babeli! Umekuwa
sehemu yakaapo mapepo, na sehemu ikaapo kila roho chafu, na sehemu akaapo kila
mchafu na ndege achukizaye. 3 Kwa kuwa mataifa yote yamekunywa mvinyo ya
tamaa ya uasherati wake ambayo humletea ghadhabu. Wafalme wa nchi wamezini
naye. Wafanyabiashara wa nchi wamekuwa matajiri kwa nguvu ya maisha yake
ya anasa.” 4 Kisha nilisikia sauti nyingine kutoka mbinguni iikisema, “Tokeni
kwake watu wangu, ili msije mkashiriki katika dhambi zake, na ili msije mkapokea
mapigo yake yoyote. 5 Dhambi zake zimerundikana juu kama mbingu, na Mungu
ameyakumbuka matendo yake maovu. 6 Mlipeni kama alivyowalipa wengine, na
mkamlipe mara mbili kwa jinsi alivyotenda; katika kikombe alichokichanganya,
mchanganyishieni mara mbili kwa ajili yake. 7 Kama alivyojitukuza yeye mwenyewe,
na aliishi kwa anasa, mpeni mateso mengi na huzuni. Kwa kuwa husema moyoni
mwake, 'Nimekaa kama malkia; wala siyo mjane, na wala sitaona maombolezo.'
8 Kwa hiyo ndani ya siku moja mapigo yake yatamlemea: kifo, maombolezo, na njaa.
Atateketezwa kwa moto, kwa kuwa Bwana Mungu ni mwenye nguvu, na ni mhukumu
wake.” 9 Wafalme wa nchi waliozini na kuchanganyikiwa pamoja naye watalia na
kumwombolezea watakapouona moshi wa kuungua kwake. 10 Watasimama mbali
naye, kwa hofu ya maumivu yake wakisema, “Ole, ole kwa mji mkuu, Babeli, mji
wenye nguvu! Kwa saa moja hukumu yako imekuja.” 11 Wafanyabiashara wa
nchi lieni na kuomboleza kwa ajili yake, kwa kuwa hakuna hata mmoja anunuaye

bidhaa zake tena - 12 bidhaa za dhahabu, fedha, mawe ya thamani, lulu, kitani
nzuri, zambarau, hariri, nyekundu, aina zote za miti ya harufu nzuri, kila chombo
cha pembe za ndovu, kila chombo kilichotengenezwa kwa miti ya thamani, shaba,
chuma, jiwe, 13 mdalasini, viungo, uvumba, manemane, ubani, mvinyo, mafuta,
unga mzuri, ngano, ng'ombe na kondoo, farasi na magari, na watumwa, na roho za
watu. 14 Matunda uliyoyatamani kwa nguvu zako yameondoka kutoka kwako. Anasa
zako zote na mapambo yametoweka, hayatapatikana tena. 15 Wafanyabiashara wa
vitu hivi waliopata utajiri kwa mapenzi yake watasimama mbali kutoka kwake kwa
sababu ya hofu ya maumivu yake, wakilia na sauti ya maombolezo. 16 Wakisema,
“Ole, ole mji ule mkuu uliovikwa kitani nzuri, zambarau, na nyekundu, na kupambwa
kwa dhahabu, na vito vya thamani na lulu!” 17 Ndani ya saa moja utajiri wote
huo ulitoweka. Kila nahodha wa meli, kila baharia, na wote wanamaji, na wote
wafanyao kazi baharini, walisimama mbali. 18 Walilia walipouona moshi wa kuungua
kwake. Walisema, “Ni mji gani unafanana na mji huu mkubwa?” 19 Walitupa
mavumbi juu ya vichwa vyao, na walilia, wakitokwa machozi na kuomboleza, “Ole,
ole mji mkubwa mahali wote waliokuwa na meli zao baharini walikuwa matajiri
kutokana na mali zake. Ndani ya saa moja umeangamizwa.” 20 “Furahini juu
yake, mbingu, ninyi waumini, mitume, na manabii, kwa maana Mungu ameleta
hukumu yenu juu yake!” 21 Malaika mwenye nguvu aliinua jiwe kama jiwe kuu
la kusagia na alilitupa baharini, akisema, “Kwa njia hii, Babeli, ule mji mkuu,
utatupwa chini kwa ukatili na hautaonekana tena. 22 Sauti ya vinanda, wanamuziki,
wacheza filimbi, na tarumbeta hawatasikika tena kwenu. Wala fundi wa aina yoyote
hataonekana kwenu. Wala sauti ya kinu haitasikika tena kwenu. 23 Mwanga wa
taa hautaangaza ndani yako. Sauti ya bwana harusi na bibi harusi hazitasikiwa tena
ndani yako, maana wafanyabiashara wako walikuwa wakuu wa nchi, na wa mataifa,
wamedanganywa kwa uchawi wako. 24 Ndani yake damu ya manabii na waamini
ilionekana, na damu ya wote waliouawa juu ya nchi.”

# 19

1 Baada ya mambo haya nilisikia sauti kama ya mlio mkubwa wa kundi kubwa
la watu mbinguni ikisema, “Haleluya. Wokovu, utukufu, na nguvu ni vya Mungu
wetu. 2 Hukumu zake ni kweli na za haki, kwa kuwa amemhukumu kahaba mkuu
aliyeiharibu nchi kwa uzinzi wake. Amefanya kisasi kwa damu ya watumishi wake,
ambayo aliimwaga yeye mwenyewe.” 3 Kwa mara ya pili walisema, “Haleluya! Moshi
hutoka kwake milele na milele.” 4 Wale wazee ishirini na wanne na viumbe hai
wanne wakasujudu na kumwabudu Mungu akaaye kwenye kiti cha enzi. Walikuwa
wakisema, “Amina. Haleluya!” 5 Ndipo sauti ilitoka kwenye kiti cha enzi, ikisema,
“Msifuni Mungu wetu, enyi watumishi wake wote, ninyi mnaomcha yeye, wote
wasio na umuhimu na wenye nguvu.” 6 Ndipo nilisikia sauti kama sauti ya kundi
kubwa la watu, kama sauti ya ngurumo ya maji mengi, na kama ngurumo ya radi,
ikisema, “Haleluya! Bwana ni Mungu wetu, mtawala juu ya wote, hutawala. 7 Na
tushangilie na kufurahi na kumpa utukufu kwa sababu harusi na sherehe ya Mwana
Kondoo imekuja, na bibi harusi yuko tayari.” 8 Aliruhusiwa kuvalishwa kitani safi
na yenye kung'aa (kitani safi ni matendo ya haki ya waumini). 9 Malaika akasema
nami, “Yaandike haya: Wamebarikiwa walioalikwa kwenye sherehe ya harusi ya
Mwana kondoo.” Vilevile akaniambia, “Haya ni maneno ya kweli ya Mungu.”
10 Nilisujudu mbele ya miguu yake nikamwabudu, lakini akaniambia, “Usifanye
hivi! Mimi ni mtumishi mwenzako na wa ndugu zako mwenye kuushika ushuhuda
wa Yesu. Mwabudu Mungu, kwa kuwa ushuhuda wa Yesu ni roho ya unabii.”
11 Kisha niliona mbingu zimefunguka, na tazama kulikuwa na farasi mweupe! Na

yule aliyekuwa amempanda anaitwa Mwaminifu na wa Kweli. Huhukumu kwa
haki na kufanya vita. [12] Macho yake ni kama mwali wa moto, na juu ya kichwa
chake ana taji nyingi. Ana jina lililoandikwa juu yake asilolifahamu mtu yeyote
isipokuwa yeye mwenyewe. [13] Amevaa vazi lililochovywa katika damu, na jina
lake aliitwa Neno la Mungu. [14] Majeshi ya mbinguni yalikuwa yakimfuata juu ya
farasi weupe, walivalishwa kitani nzuri, nyeupe na safi. [15] Kinywani mwake hutoka
upanga mkali ambao huyaangamiza mataifa, naye atawatawala kwa fimbo ya chuma.
Naye hukanyaga vyombo vya mvinyo kwa hasira kali ya Mungu, hutawala juu ya
wote. [16] Naye ameandikwa juu ya vazi lake na katika paja lake jina, MFALME WA
WAFALME NA BWANA WA MABWANA. [17] Niliona malaika amesimama katika jua.
Aliwaita kwa sauti kuu ndege wote warukao juu, “Njoni, kusanyikeni pamoja kwenye
chakula kikuu cha Mungu. [18] Njoni mle nyama ya wafalme, nyama ya majemedari,
nyama ya watu wakubwa, nyama ya farasi na wapanda farasi, na nyama ya watu
wote, walio huru na watumwa, wasio na umuhimu na wenye nguvu.” [19] Nilimwona
mnyama na wafalme wa nchi pamoja na majeshi yao. Walikuwa wamejipanga kwa
ajili ya kufanya vita na mmoja aliyepanda farasi na jeshi lake. [20] Mnyama alikamatwa
na nabii wake wa uongo aliyezifanya ishara katika uwepo wake. Kwa ishara hizi
aliwadanganya wale walioipokea chapa ya mnyama na walioisujudia sanamu yake.
Wote wawili walitupwa wangali hai katika ziwa la moto liwakalo kwa kiberiti. [21] Wale
waliobaki waliuawa kwa upanga uliotoka kinywani mwa mmoja aliyepanda juu ya
farasi. Ndege wote walikula mizoga ya miili yao.

# 20

[1] Kisha niliona malaika akishuka kutoka mbinguni, akiwa na ufunguo wa shimo
lisilo na mwisho na mnyororo mkubwa mkononi mwake. [2] Alimshika yule joka,
nyoka wa zamani, ambaye ni ibilisi au Shetani, na kumfunga miaka elfu. [3] Alimtupa
kwenye shimo lisilo na mwisho, akalifunga na kulitia mhuri juu yake. Hii ilikuwa
hivyo ili kwamba asiwadanganye mataifa tena mpaka miaka elfu itakapoisha.
Baada ya hapo, ataachiwa huru kwa muda mchache. [4] Kisha niliona viti vya
enzi. Waliokuwa wamevikalia ni wale ambao walikuwa wamepewa mamlaka ya
kuhukumu. Vilevile niliona nafsi za wale ambao walikuwa wamekatwa vichwa kwa
ajili ya ushuhuda kuhusu Yesu na kwa neno la Mungu. Walikuwa hawajamwabudu
mnyama au sanamu yake, na walikataa kupokea alama juu ya paji za nyuso zao
au mkono. Walikuja uzimani, na wakatawala pamoja na Kristo kwa miaka elfu.
[5] Wafu waliobaki hawakuja uzimani mpaka miaka elfu ilipokuwa imeisha. Huu
ndio ufufuo wa kwanza. [6] Mbarikiwa na mtakatifu ni mtu yeyote ambaye achukua
nafasi katika ufufuo wa kwanza! Mauti ya pili haina nguvu juu ya watu kama hawa.
Patakuwa na makuhani wa Mungu na wa Kristo na watatawala na yeye kwa miaka
elfu. [7] Wakati miaka elfu itakapofikia mwisho, Shetani atafunguliwa kutoka gerezani
mwake. [8] Atakwenda nje kuwadanganya mataifa katika kona nne za dunia -Gogu
na Magogu - kuwaleta pamoja kwa ajili ya vita. Watakuwa wengi kama mchanga
wa bahari. [9] Walikwenda juu kwenye tambarare ya nchi nao walizunguka kambi ya
waumini, mji upendwao. Lakini moto ulikuja kutoka mbinguni na kuwaangamiza.
[10] Shetani, ambaye aliwadanganya, alitupwa ndani ya ziwa liwakalo kiberiti, ambamo
mnyama na nabii wa uongo walikuwa wameshatupwa. Watateswa mchana na usiku
milele na milele. [11] Kisha niliona kiti cha enzi kikubwa cheupe na yule ambaye
alikaa juu yake. Dunia na mbingu zilikimbia mbali kutoka katika uwepo wake,
lakini hapakuwako nafasi ya wao kwenda. [12] Niliwaona waliokufa - hodari na
wasio wa muhimu wamesimama katika kiti cha enzi, na vitabu vilifunuliwa. Kisha
kitabu kingine kilifunguliwa - Kitabu cha Uzima. Wafu walihukumiwa kwa kile

kilichoandikwa ndani ya vitabu, matokeo ya kile walichokifanya. 13 Bahari iliwatoa
wafu ambao walikuwa ndani yake. Kifo na kuzimu viliwatoa wafu ambao walikuwa
ndani yake, na wafu walihukumiwa kulingana na walichofanya. 14 Kifo na kuzimu
zilitupwa ndani ya ziwa la moto. Hii ni mauti ya pili - ziwa la moto. 15 Kama jina la
yeyote halikupatikana limeandikwa ndani ya Kitabu cha Uzima, alitupwa ndani ya
ziwa la moto.*

# 21

1 Kisha nikaona mbingu mpya na nchi mpya, kwa kuwa mbingu ya kwanza na
nchi ya kwanza zimekwishapita, na bahari haikuwepo tena. 2 Niliona mji mtakatifu,
Yerusalemu mpya, ambao ulikuja chini kutoka mbinguni kwa Mungu, ulioandaliwa
kama bibi harusi aliyepambwa kwa ajili ya mumewe. 3 Nilisikia sauti kubwa
kutoka kwenye kiti cha enzi ikisema, “Tazama! Makao ya Mungu yapo pamoja na
wanadamu, naye ataishi pamoja nao. Watakuwa watu wake, na Mungu mwenyewe
atakuwa nao na atakuwa Mungu wao. 4 Atafuta kila chozi kutoka katika macho
yao, na hapatakuwa na kifo tena, au kuomboleza, au kulia, au maumivu. Mambo
ya zamani yamekwishakupita. 5 Yeye ambaye alikuwa ameketi juu ya kiti cha enzi
alisema, “Tazama! Nafanya mambo yote kuwa mapya.” Alisema, “Andika hili
kwa sababu maneno haya ni ya hakika na kweli.” 6 Aliniambia, “Mambo haya
yalikwisha kupita! Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho. Kwa yeyote
aonaye kiu nitampatia kinywaji bila gharama kutoka katika chemchemi za maji ya
uzima. 7 Yeye ashindaye atayarithi mambo haya, na nitakuwa Mungu wake, naye
atakuwa mwanangu. 8 Lakini kama ilivyo kwa waoga, wasioamini, wachukizao,
wauaji, wazinzi, wachawi, waabudu sanamu, na waongo wote, sehemu yao itakuwa
katika ziwa la moto wa kiberiti uunguzao. Hiyo ndiyo mauti ya pili.” 9 Mmoja wa
malaika saba alikuja kwangu, mmoja ambaye alikuwa na mabakuli saba yaliyojaa
mapigo saba ya mwisho na alisema, “Njoo hapa. Nitakuonesha bibi harusi, mke wa
mwana kondoo.” 10 Kisha alinichukua mbali katika Roho kwenye mlima mkubwa na
mrefu na alinionesha mji mtakatifu, Yerusalemu, ukishuka chini kutoka mbinguni
kwa Mungu. 11 Yerusalemu ulikuwa na utukufu wa Mungu, na uzuri wake ulikuwa
kama kito cha thamani, kama jiwe la kioo safi la yaspi. 12 Ulikuwa na ukuta mkubwa,
mrefu wenye milango kumi na miwili, pamoja na malaika kumi na wawili milangoni.
Juu ya milango palikuwa pameandikwa majina ya makabila kumi na mawili ya
wana wa Israeli. 13 Upande wa mashariki palikuwa na milango mitatu, upande
wa kusini milango mitatu, upande wa kaskazini milango mitatu, na upande wa
magharibi milango mitatu. 14 Kuta za mji zilikuwa na misingi kumi na miwili, na
juu yake palikuwa na majina kumi na mawili ya mitume kumi na wawili wa Mwana
Kondoo. 15 Mmoja aliyeongea nami alikuwa na kipimo cha fimbo iliyotengenezwa
kwa dhahabu kwa ajili ya kupima mji, milango yake na kuta zake. 16 Mji uliwekwa
ndani ya mraba; urefu wake ulikuwa sawa na upana wake. Alipima mji kwa
kipimio cha fimbo, stadia 12, 000 kwa urefu (urefu wake, upana, na kimo vilifanana).
17 Vilevile alipima ukuta wake, unene wake ulikuwa dhiraa 144 kwa vipimo vya
kibinadamu (ambavyo pia ni vipimo vya malaika). 18 Ukuta ulikuwa umejengwa
kwa yaspi na mji wenye dhahabu safi, kama kioo safi. 19 Misingi ya ukuta ilikuwa
imepambwa na kila aina ya jiwe la thamani. La kwanza lilikuwa yaspi, la pili lilikuwa
yakuti samawi, la tatu lilikuwa kalkedon, la nne zumaridi, 20 la tano sardoniki, la
sita akiki, la saba krisolitho, la nane zabarajadi, la tisa yakuti ya manjano, la kumi
krisopraso, la kumi na moja hiakintho, la kumi na mbili amethisto. 21 Milango kumi
na miwili ilikuwa lulu kumi na mbili, kila mlango ulitengenezwa kutoka kwenye
lulu moja. Mitaa ya mji ilikuwa dhahabu safi, ikionekana kama kioo safi. 22 Sikuona

hekalu lolote ndani ya mji, kwa kuwa Bwana Mungu, ambaye anatawala juu ya vyote,
na Mwana Kondoo ni hekalu lake. [23] Mji haukuhitaji jua au mwezi ili kungaza juu
yake kwa sababu utukufu wa Mungu uliangaza juu yake, na taa yake ni Mwana
Kondoo. [24] Mataifa watatembea kwa mwanga wa mji huo. Wafalme wa dunia
wataleta fahari zao ndani yake. [25] Milango yake haitafungwa wakati wa mchana, na
hapatakuwa na usiku pale. [26] Wataleta fahari na heshima ya mataifa ndani yake,
[27] na hakuna kichafu kitakachoingia ndani yake. Wala yeyote ambaye afanyaye
jambo lolote la aibu au udanganyifu hataingia, bali ni wale tu ambao majina yao
yameandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana Kondoo.

## 22

[1] Kisha malaika akanionesha mto wa maji ya uzima, maji yalikuwa ya mng'ao
kama wa bilauri. Yalikuwa yakitiririka kutoka katika kiti cha enzi cha Mungu na
cha Mwana Kondoo [2] Kupitia katikati ya mtaa wa mji. Katika kila pembe ya mto
palikuwa na mti wa uzima, unaozaa aina kumi na mbili za matunda, na huzaa
matunda kila mwezi. Majani ya mti ni kwa ajili ya uponyaji wa mataifa. [3] Wala
hapatakuwa na laana yoyote tena. Kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana Kondoo
kitakuwemo ndani ya mji, na watumishi wake watamtumikia. [4] Watamuona uso
wake, na jina lake litakuwa juu ya vipaji vya nyuso zao. [5] Hapatakuwa na usiku
tena; wala hapatakuwa na hitaji la mwanga wa taa au jua kwa sababu Bwana
Mungu ataangaza juu yao. Nao watatawala milele na milele. [6] Malaika akaniambia,
“Maneno haya ni ya kuaminika na kweli. Bwana Mungu wa roho za manabii
alimtuma malaika wake kuwaonesha watumishi wake kitakachotokea hivi karibuni.”
[7] “Tazama! Ninakuja upesi! Amebarikiwa yeye anayeyatii maneno ya unabii wa
kitabu hiki.” [8] Mimi, Yohana, ndiye niliyesikia na kuona mambo haya. Nilipoyasikia
na kuyaona, nilianguka chini mwenyewe mbele ya miguu ya malaika kumwabudu,
malaika aliyenionesha mambo haya. [9] Akaniambia, “Usifanye hivyo! Mimi ni
mtumishi mwenzako, pamoja na ndugu zako manabii, pamoja na wale wanaotii
maneno ya kitabu hiki. Mwabudu Mungu!” [10] Akaniambia, “Usiyatie muhuri maneno
ya unabii wa kitabu hiki, maana wakati umekaribia. [11] Asiye mwenye haki, aendelee
kutokuwa mwenye haki. Ambaye ni mchafu kimaadili, na aendelee kuwa mchafu
kimaadili. Mwenye haki, na aendelee kuwa mwenye haki. Aliye mtakatifu, na
aendelee kuwa mtakatifu.” [12] “Tazama! Naja upesi. Ujira wangu uko pamoja nami,
kumlipa kila mmoja kulingana na alichokifanya. [13] Mimi ni Alfa na Omega, wa
Kwanza na wa Mwisho, Mwanzo na Mwisho. [14] Wamebarikiwa wale waoshao mavazi
yao ili kwamba wapate haki ya kula kutoka katika mti wa uzima na kuuingia mji
kupitia malangoni. [15] Nje kuna mbwa, wachawi, wazinzi, wauwaji, waabudu sanamu,
na kila apendaye na ashuhudiaye ushahidi wa uongo. [16] Mimi, Yesu, nimemtuma
malaika wangu kuwashuhudia kuhusu mambo haya kwa makanisa. Mimi ni mzizi
wa uzao wa Daudi, Nyota ya Asubuhi ing'aayo.” [17] Roho na Bibi harusi asema, “Njoo!”
Na yeye asikiaye aseme, “Njoo!” Yeyote aliye na kiu, na aje, na yeyote anayetamani,
na apate maji ya uzima bure. [18] Namshuhudia kila mtu asikiaye maneno ya unabii
wa kitabu hiki: Kama yeyote ataongeza katika hayo, Mungu atamuongezea mapigo
yaliyoandikwa katika kitabu hiki. [19] Kama mtu yeyote atayaondoa maneno ya kitabu
hiki cha unabii, Mungu ataondoa sehemu yake katika mti wa uzima na katika
mji mtakatifu, ambayo habari zake zimeandikwa ndani ya kitabu hiki. [20] Yeye
ashuhudiaye mambo haya asema, “Ndiyo! Naja upesi.” Amina! Njoo, Bwana Yesu!
[21] Neema ya Bwana Yesu iwe na kila mtu. Amina.